

QUR'AN TUKUFU

Pamoja na Tafsiri na Maelezo kwa

KISWAHILI

The Holy Qur'an with Swahili Translation

Translator: **Maulana Sheikh Mubarak Ahmad Ahmadi H.A.**
© **Islam International Publication**
16, Gressenhall Road
SW 18 5QL
London
Published by: **Ahmadiyya Muslim Jamaat Tanzania**
P. O. Box 376 Dar es Salaam
Tel: 022 - 2110473 Fax 022 - 2121744

ISBN

HAKI ZOTE ZIMEHIFADHIWA

Chapa ya Kwanza	*1953*	*Nakala 10,000*	*Nairobi*
Chapa ya Pili	*1971*	*Nakala 5,000*	*Rabwah*
Chapa ya Tatu	*1981*	*Nakala 10,000*	*London*
Chapa ya Nne	*1991*	*Nakala 5,000*	*Dar es Salaam*
Chapa ya Tano	*2002*	*Nakala 10,000*	*Nairobi*
Chapa ya Sita	*2013*	*Nakala 10,000*	*London*



تَنْزِيْلٌ مِّنْ رَّبِّ الْعٰلَمِيْنَ

QUR'AN TUKUFU

PAMOJA NA TAFSIRI NA MAELEZO KWA KISWAHILI

Imefasiriwa na

SHEIKH MUBARAK AHMAD AHMADI H.A

Rais-ut-Tabligh na Amir wa zamani wa

JUMUIYA YA WAISLAM WA AHMADIYYA KATIKA AFRIKA MASHARIKI

CHAPA YA SITA

2013

NENO LA MBELE

Kwa jina la Allah, Mwingi wa Rehema, Mwingi wa Ukarimu

Ninayo furaha kubwa kuweka mbele yenu chapa ya sita ya tafsiri ya Qur'an Tukufu kwa lugha ya Kiswahili. Baada ya kupata malalamiko kadhaa kutoka kwa ndugu mbalimbali, ya kuwepo kwa baadhi ya makosa ndani ya tafsiri ya toleo lililopita, nilimwomba kiongozi wetu mkuu wa Jumuiyya ya Waislamu wa Ahmadiyya duniani – Hadhrat Mirza Masroor Ahmad, Khalifatul Masih wa tano, Mwenyezi Mungu Amsaidie kwa Roho Mtakatifu na kumjaalia umri mrefu – juu ya haja ya kupitiwa upya tafsiri yote. Ndipo Khalifa Mtukufu a.t.b.a. akaidhinisha kamati maalum ya kulishughulikia suala hilo. Khalifa Mtukufu aliidhinisha kamati iliyowajumuisha:

1. Sheikh Bakri Abedi Kaluta, Mkuu wa Dawati la Kiswahili.
2. Sheikh Asif Mahmood Butt, Mbashiri wa mkoa wa Morogoro na mjumbe wa Dawati la Kiswahili.
3. Sheikh Karim ud din Shams, Mkuu wa Jamia Ahmadiyya.
4. Halikadhalika Sheikh Hadayatullah Hubsch alitoa mchango mkubwa kuweka matini mpya ya maandiko ya Kiarabu ya Kurani Tukufu.

Pia tulipata maagizo toka Makao Makuu ya kufanya masahihisho kwa kuizingatia tafsiri ya Qur'an Tukufu iliyotafsiriwa na Hadhrat Khalifatul Masih IV rh.a. kwa lugha ya Kiurdu. Kwa hiyo kuna baadhi ya mabadiliko yatakayoonekana humo yaliyosababishwa na uzingatiaji wa tafsiri hiyo nzuri ya Kiurdu. Kazi hii imechukua muda wa takriban miaka miwili. Twamshukuru Allah Aliyewezesha ufanikishaji wa shughuli hii muhimu yenye baraka. Namwomba Mwenyezi Mungu Mtukufu, Awalipe malipo mema wale wote walioshiriki katika shughuli hii kwa namna moja au nyingine – Amin.

Tahir Mahmood Chaudhry,
Amir na Mbashiri Mkuu,
Jumuiya ya Waislamu wa Ahmadiyya, Tanzania.
September 25, 2013



DIBAJI*

Tafsiri ya Qur'an Tukufu na maelezo machache juu ya madhumuni yake inatangazwa kwa lugha ya Kiswahili.

Kwa hakika Afrika ina heshima maalum katika historia ya Kiislamu, hasa Afrika ya kaskazini-ya-mashariki. Katika siku za mwanzo za Uislamu, watu wa Makka walipowadhulumu Waislamu kwa dhuluma kubwa, na kukaa kwa Waislamu katika Makka kukawa hakuwezekani, Mtume (sallallaahu 'alaihi wasallam)** kwa amri ya Allah, aliwaagiza Waislamu wahame na kwenda nchi ya Uhabeshi.

Uhabeshi ndiyo Abisinia ambayo mipaka yake inaungana na Kenya. Waislamu walipofika katika nchi hiyo, na kwa mujibu wa sheria na kanuni ya nchi ile, hawakupewa taabu wala udhia, na wakaanza kupata pumzi ya raha na amani, hapo watu wa Makka hawakuweza kuvumilia, wakawatuma viongozi wawili wa kaumu yao, pamoja na zawadi na hidaya nyingi kwa ajili ya mfalme na wakuu wa baraza lake. Wakawaagiza wajumbe wao waombe kwa mfalme ya kwamba hao wahamaji waliotoka Makka waliomo katika nchi yake watolewe na kurudishwa kwa serikali ya Makka, ili serikali ya Makka iwatendee sawa na maoni na itikadi zao. Na kama mfalme asikubali, wawatumie wakuu wa baraza la mfalme kwa kuwapa zawadi ili wambembeleze na kumshawishi mfalme awafukuze Waislamu waliohama kutoka Makka, na kwa njia yo yote warudishwe na kupelekwa Makka.

Wajumbe hao walifika huko Uhabeshi, na wakawatumia wakuu wa baraza, hasa mapadre, na wakaonana na mfalme aliyekuwa siku zile akiitwa Negus, na Waarabu walikuwa wakimwita Najashi. Jina hili kwa hakika halikuwa jina hasa la mfalme huyo, bali lilikuwa lakabu ya wafalme wa kihabeshi wa siku zile.

Wajumbe wa Makka walishtaki kwa mfalme ya kuwa baadhi ya waasi wa nchi yao wametoroka na kukimbilia Uhabeshi, nao wametumwa na watu wa Makka ili waasi hao warudishwe kwa serikali ya Makka.

Mfalme aliposikia maombi yao, akawaita Waislamu na kuwauliza: "Mmefikaje hapa?" Wakajibu ya kuwa watu wa nchi yao walikuwa wakiwadhulumu. Na adili na unyofu wa mfalme wa Kiafrika ulivuma sana. Basi hawakuwa na njia ila kukimbilia katika nchi yake.

Hapo mfalme akawajibu wajumbe wa Makka ya kuwa yeye hakuona kosa lao katika mambo ya utawala, isipokuwa wanahitilafiana mambo ya dini, na hivyo, hakuona njia ya kuwarudisha.

---

*Dibaji hii imeandikwa na Seyidna Amir-ul-Muuminiin, Hadhrat Mirza Bshir-ud-Din Mahmud Ahmad, Khalifat-ul-Masih II, Kiongozi Mkuu wa Mwendeleo wa Ahmadiyya katika Uislamu. Aliandika kwa lugha ya Kiurdu, nasi tumeifasiri kwa Kiswahili.

** Utakuta maneno haya yamefupishwa kwa kuandikwa *s.a.w.* Maana ya maneno haya ni "Amani na rehema za Allah juu yake." Kila anapotajwa Mtume Muhammad maneno haya ambayo ni maombi kwa ajili yake, hutamkwa na msemaji na pia wanaosikia.

Wajumbe wa Makka walipotoka katika baraza hali wameshindwa, wakagawanya zawadi kwa wakuu wa baraza na mapadre. Na wakawachochea kwa kuwaambia ya kuwa hao Waislamu walimtukana hata Yesu Masihi, kwa hiyo Wakristo pia walitakiwa kuungana na watu wa Makka katika kuwataabisha Waislamu.

Siku ya pili, wakuu wa baraza wakamhimiza mfalme na kumkazania kwa kumwambia ya kuwa hao Waislamu hata wanamtukana Masihi pia.

Mfalme akawaita Waislamu tena na kuwauliza wana itikadi gani juu ya Masihi.

Hapo Waislamu wakamsomea Aya za mwanzo za sura Maryam ambazo zinaeleza habari za Masihi (amani ya Mungu juu yake) na mama yake. Baada ya kuzisoma Aya hizo wakasema, "Sisi tunaamini ya kuwa Masihi ni Nabii wa Allah, ila hatuamini kuwa yeye ni mwana wa Allah."

Lo! mapadre waliposikia hivi, wakapiga makelele. "Tazameni hawa wanamtukana Masihi!" Lakini mfalme Mwafrika alikuwa ni mwadilifu na mwenye haki, akajua mara moja ya kuwa Waislamu wanasingiziwa bure, wao wanamheshimu Masihi, ila hawamkubali kuwa Mungu au mwana wa Mungu. Hapo akapandwa na jadhba, na akaokota jani moja katika sakafu, na akasema: "Kwa haki ya Allah mimi pia namwamini Masihi jinsi wanavyomwamini hawa Waislamu, na cheo walichompa wao, mimi simpi zaidi hata sawa na jani hili."

Mapadre waliposikia hukumu ya mfalme, wakaanza kumzomea na kumwambia ameacha dini. Lakini Najashi alisema, "Sitaghilibiwa na zahama yenu, wala sitaogopa makelele yenu. Baba yangu alipofariki nilikuwa bado mtoto mdogo, na amu yangu aliwekwa kuwa mfalme kama naibu wangu na ninyi kwa kupatana naye mlishauriana kuninyima ufalme. Nilipojua jambo hili, ingawa nilikuwa mtoto nilitaka kupata haki yangu, na vijana wakaungana nami, na amu yangu kwa kuogopa akajiuzulu na akanipa ufalme. Basi ufalme wangu sikuupata kwa msaada wenu, bali Allah ndiye aliyenisaidia na kunipa, ingawa ninyi mlifanya juhudi ya kuninyang'anya. Je, sasa kwa kuwaogopeni ninyi nimwache Allah na nishike dhuluma na jeuri? Hamkunipa ufalme, wala sina haja ya kuomba msaada kwenu, na kwa hali yo yote ile, siwezi kufanya dhuluma. Hao watakaa katika nchi yangu kwa uhuru, na hakuna atakayeweza kuwadhuru."

Basi, enyi watu wa Afrika ambayo sehemu yake ya mashariki ina lugha ya elimu - Kiswahili, kwa kuweka mbele yenu tafsiri hii naona ladha na furaha, maana katika siku za mwanzo wa Kitabu hiki, bara lenu liliwalinda wale waliokiamini Kitabu hiki na likakataa kabisa kuwatendea dhuluma na jeuri, bali likakazana kusimamisha Uadilifu na haki. Leo mafundisho matakatifu ya Qur'an yako katika hali ya kudhulumiwa kama walivyokuwa wakidhulumiwa walioiamini Qur'an.

Kweli Nabii aliyeileta Qur'an Tukufu katika dunia amekwisha kufa, lakini kuwapo kwake kwa kiroho leo kunadhulumiwa zaidi kuliko alivyokuwepo miaka 1,400 kabla, alipokuwa akidhulumiwa katika maisha yake ya kimwili. Yeye anasingiziwa, na mafundisho yake yanaelezwa na yanawekwa mbele ya dunia kwa sura mbaya. Na wanaomwamini yeye wanafahamiwa kuwa ni wanyonge na dhalili. Lakini Allah Anaona ya kuwa hayo si haki. Mtakatifu na mwenye heshima zaidi katika macho ya Allah ni Mtume

Muhammad s.a.w. ambaye ilimshukia Qur'an hii; na mafundisho yenye haki zaidi ni yale yaliyomo katika Kitabu hiki, yaani Qur'an Tukufu, na ninyi mtayaona wenyewe.

Dunia, katika ghururi na nguvu na uwezo wake, inashughulika kuyapinza mafundisho yake, na inaendelea kuwafedhehesha wanaokiamini Kitabu hiki. Lakini, enyi watu wa Afrika, hata ninyi pia mko katika hali ya namna hii. Wacheni nchi za kigeni, hata katika nchi yenu wenyewe ninyi hamheshimiwi. Hivyo, mafundisho yaliyowapandisha watu miaka elfu moja na mia nne kabla ya leo, waliokuwa hawajastaarabika, wasio na maarifa wala elimu, kwenye vilele vya maendeleo ya kila namna ya dunia, lakini yamekuwa katika hali ya kudhulumiwa, na yametiwa umaskini na ufukara - mafundisho haya nayaweka mbele yenu ninyi ambao hali yenu ni ya nmna hii hii, nami nawatakeni mkisome Kitabu hiki kwa kutafakari, na mkitazame kwa macho ya uadilifu na wema ule ule kama alivyofanya mfalme Mwafrika, Najashi, alipowaona Waislamu waliohamia katika nchi yake.

Tena mkitazame kwa akili yenu na busara yenu, wala msiingiwe na athari ya masingizio ya uwongo waliyoleta watu, wala msikitazame kwa miwani ya rangi mbalimbali iliyotengenezwa na watu.

Nina yakini kama mtafanya hivyo, bila shaka mtaijua thamani ya kito hiki kisichokuwa na mfano; mtaishika kamba aliyoiteremsha Allah kwa njia ya Kitabu hiki kitakatifu kutoka mbinguni, ili watumishi Wake kwa kuishika wafike Kwake.

Enyi watu wa Afrika! Onyesheni tena dalili ya Uadilifu na wema wenu, na toeni msaada kwa kuusimamisha ukweli - ukweli alioutuma Mwumba wenu, Allah, ambao pasipo kuukubali mataifa yaliyomo utumwani hayawezi kupata uhuru, na wanaodhulumiwa hawawezi kuokoka katika dhuluma, na wafungwa hawawezi kutoka katika magereza. Nawafikishieni ujumbe wa amani, ustawi na maendeleo. Ujumbe huu si wangu, bali ni ujumbe wa Allah Ambaye ni Mwumba wenu na Mwumba wangu. Huu ni ujumbe wa Allah Ambaye ni Mwumba wa mbingu na ardhi. Huu ni ujumbe wa Allah Ambaye ni Mwumba wa Ulaya na Amerika na Asia.

Njooni. Njooni kwa maelfu. Bali njooni kwa malaki. La, bali njooni kwa mamilioni, mkusanyike chini ya bendera ya ukweli, ili sisi sote, kwa kuungana pamoja, tuusimamishe tena ufalme wa Allah, na tusimamishe undugu wa wanadamu ulimwenguni, na tusimamishe Uadilifu na wema katika dunia.

Allah Awapeni nguvu na uwezo wa kuitikia wito wangu, nami nipate kuiona siku ambayo ninyi mtasimama pamoja nami, bega kwa bega, tukiendelea na juhudi ya kusimamisha amani, usalama, maendeleo na ustawi duniani. Na mwishowe juhudi hii ifanikiwe kwa baraka na fadhili za Allah.

MIRZA MAHMUD AHMAD
KHALIFAT-UL-MASIH

Rabwah (Pakistan)
17 Januari, 1953.

MAJINA YA VITABU TULIVYOREJEA

Vitabu tulivyorejea mara kwa mara katika tafsiri hii tumeviandika kwa kifupi tu katika maelezo. Vichache tumevitaja kwa ukamilifu. Bado kuna vingine tulivyorejea lakini hatukuvitaja katika maelezo. Hapa tunataja majina ya vitabu hivyo na pengine majina ya walioviandika pia.

Vitabu vya Tafsiri za Qur'an

Jarir . . . . . Tafsiri ibni Jarir, cha Imam Abu Ja'far Muhammad ibni Jarir
Tabari Kathir . . . Cha Abul Fida Ismail ibni al-Kathir.
Kashshaf . . . . . Al-Kashshaf 'an Ghawaamidh at-Tanzil, cha Imam Mahmud bin Umar Zamakhshari.
Muhit . . . . . Al-Bahrul-Muhit, cha Athiirud-Din Abu Abdullah Muhammad ibni Yusuf wa Granada (Spain) aitwaye Abu Hayyan.
Manthur . . . . . Durri Manthur, cha Hafidh Jalal-ud-Din Abdur-Rahman Suyuti
Maani . . . . . Ruhul-Ma'ani, cha Abdul Fadhil Shihabud-Din Mahmud al-Baghdad.
Baidhawi . . . . . Anwar-ut-Tanzil, cha Kadhi Nasirud-Din Abu Sa'id Baidhawi.
Bayan . . . . . Ruhul-Bayan, cha Sheikh Ismail Haqqi.
Razi . . . . . At-Tafsiirul-Kabiir, cha Imam Muhammad Fakhrud-Din Razi.
Majma'ul Bahrain . . Cha Hafidh Jalal-ud-Din Abdul-Rahman Suyuti.
Swaafii . . . . . Tafsiir Swaafii ya madhehebu ya Kishia.
Jaami'ul Bayan . . Cha Imam Abu Ja'far Muhammad ibni Jarir Twabari.
Sawi . . . . . Cha Ahmad bin Muhammad As-Sawi.
Jalalein . . . . . Cha Jalal-ud-Din Muhammad bin Ahmad na Hafidh Jalal-ud-Din Abdu-Rahman Suyuti.

Tafsiri Ma'alim Tanzil, Abu Muhammad Husain bin Mas'ud, Al-Farraa, Al-Baghvi.
The Holy Quran with English Translation and Commentary Vol. I & II published by the Sadr Anjuman Ahmadiyya, Rabwah, Pakistan.
Tafsir Kabiir, cha Hadhrat Mirza Bashir-ud-Din Mahmud Ahmad (Khalifat-ul-Masih II).
Tafsir-ul-Quran, cha Maulana Seyyid Muhammad Sarwar Shah.
Tafsir-ul-Quran, cha Hafidh Roshan Ali.
Tafsir-ul-Quran cha 'Allama Seyyid Muhammad Is'haq.
The Holy Quran, by Maulana Muhammad Ali M.A., LL.B., Lahore, Pakistan.
Translation of the Holy Quran, by Al-Haj Hafidh Ghulam Sarwar, M.A., B.A.
The Koran, by Rev. J. M. Rodwell, M. A.
The Koran, by George Sale.
Translation of the Holy Quran, by Abdullah Yusuf Ali.
Tafsiri ya Qur'an ya Kiarabu, cha Godfrey Dale, Zanzibar.

Tafsiri ya Juzu Alif Laam Miim, cha Sheikh Al-Amin bin Ali, Mombasa.
Tafsiri ya Baadhi ya Sura za Qurani: Yasin, Waqia, Mulk, cha Sheikh Abdallah Saleh Al-Farsy, Zanzibar.
Introduction to the Study of the Holy Quran, by Hadhrat Mirza Bashir-ud-Din Mahmud Ahmad (Khalifatul Masih II).

Vitabu vya Hadithi za Mtume s.a.w.

Bukhari	Sahihi Bukhari, cha Abu Abdullah Muhammad bin Ismail Bukhari.
Muslim	Sahih Muslim, cha Hafidh Abul Husain Muslim bin Hajjaj al- Qushairi.
Tirmidhi.	Jami' Tirmidhi, cha Abu Isa Muhammad bin Isa Tirmidhi.
Dawud (au Abu Dawud) .	Sunan Abu Dawud, cha Hafidh Sulaiman bin Ash'ath Abu Dawud
Majah	Sunan Ibni Majah, cha Muhammad bin Yazid Abu Abdullah ibni Majah Qazwini.
Musnad	Musnad Ahmad bin Hanbal, cha Imam Abu Abdullah Ahmad bin Hanbal.
Mu'atta	Cha Imam Malik.
Baihaki	Sunan Baihaqi, cha Abu Bakar Ahmad bin Husain al-Baihaqi.
'Ummaal	Kanzul-'Ummaal fi Sunanil-Aqwaal wal Af'aal, cha Hafidh 'Ala-ud-Din Ali al-Muttaqi.
Kutni.	Sunan Dar Qutni, cha Hafidh Ali bin Umar al-Dar Qutni.
Qastalani	Irshaad-us-Saari, cha Ahmad bin Muhammad al-Khatib Qastalani.
Nasai.	Sunan Nasai, cha Hafidh Abu Abdur-Rahamn Ahmad bin Shu'aib Nasai.
Saghir	Al-Jaami'us-Saghiir fi Ahaadiithil-Bashiirin-Nadhiir.
Asakir	Ibni 'Asakir, cha Abul Qasim Ali bin Al Hasan ibni 'Asakir.
Tahawi	Sharh Ma'aanul-Aathar, cha Ja'far at-Tahawi.
Mishkat	Mishkaatul-Masaabih, cha Sheikh Waliyud-Din Muhammad Abdullah.
Kashful-Ghummah . . .	Kashful-Ghummah 'an Jamii'il Ummah, cha Imam Abul-Mawaahib Abdul-Wahhaab bin Ahmad bin Ali Ashsha'rani.

Makamusi, Ma-Encyclopaedia na Magazeti

Bihar . . . . . Takmil Majma' Biharul-Anwar, cha Sheikh Muhammad Tahir Gujrati.
Baka . . . . . Kulliyaat, cha Abul Baqaa.
Mufradat . . . . . Al-Mufradaat fi Gharibil-Qur'an, cha Sheikh Abul Qasim Muhammad bin Mukarram.
Taj . . . . . Tajul-'Arus, cha Abul Fadhil Sayyid Muhammad Murtadha al-Husaini.
Kamus . . . . . Qaamus, cha Sheikh Nasr Abul Wafaa.
Akrab . . . . . Aqrabul-Mawaarid, cha Sa'id al-Khauri al-Shartuti.
Munjid . . . . . Cha Al-Ab Lewis
Lane . . . . . Arabic - English Lexicon, by E. W. Lane.
Enc. Bri. . . . . Encyclopaedia Britanica, 14th edition.
Enc. Rel. Eth. . . . . Encyclopaedia of Religion and Ethics.
Jew. Enc. . . . . Jewish Encyclopaedia.
Encyclopaedia of Religious Knowledge.
Encyclopaedia Biblica.
Encyclopaedia of Religion and Religions by Royston Pike.
Buck's Theological Dictionary.
Arrisaalat war-Riwaayat, Cairo (Misri).
The East African Standard, Nairobi.
The Review of Religions, Rabwah, Pakistan.
Alhakam, Qadian.
Alfadhl, Qadian.
Alfurqan, Ahmadnagar, Rabwah.

Vitabu vya Jografia na Historia

Tabari . . . . . Taariikh-ur-Rasul wal-Muluuk, cha Abu Ja'far Muhammad bin Jarir.
Hisham . . . . . Siiratun-Nabii, cha Sheikh Abu Muhammad Abdul Malik ibni Hisham.
Khamis . . . . . Taariikhul Khamiis, cha Sheikh Husain ibni Muhammad ad-Diyar al-Bakri.
Zurkani . . . . . Sharh Zurqani, cha Imam Muhammad ibni Abdul Baaqi az-Zurqaani.
Mu'jam . . . . . Mu'jamul-Buldan, cha Abu Abdullah Yaqut bin Abdullah al-Baghdadi.

Futuuhul Buldaan, cha Balaadhari.
Muruuj adh-Dhahab wa Ma'aadinul-Jauhar, cha 'Allama Abul Hasan Ali bin Husain al-Mas'udi.
Mawaahibul-Ladunniyya, cha Shihabud-Din Ahmad Qastalani.
Ibni Is'haaq.
Siirat Khaatamannabiyyiin, cha Hadhrat Mirza Bashir Ahmad, M.A. Qadiani.
Life of Muhammad, by Sir William Muir, K.C.S.I (1923).
The Caliphate, its Rise and Decline and Fall, by Sir William Muir K.C.S.I.
Dowlings History of Romanism.
Historians History of the World.
Histories of the Reformation.
Preaching of Islam, by T.W. Arnold.
The Muslim World.
The World of the Arabs.
Oswald's Kingdom.
The Hakluyt Society, London.
The War of the Huguenots.
The New Congo, by Tom Marvel, New York.
Tropical Africa in World History, by T. R. Batten, Makerere College, Uganda.
Fox Book of Martyrs.
Gibbon's Roman Empire vol. v.
Cherlote Elizabeth's Martyrology.
Butler's Arab Conquest of Egypt.
The Great Red Dragon.
Christianity in Africa, by Diedrich Westermann.
Counquest of Mexico.
Jinsi Dini ya Kiislamu ilivyotungwa, cha Rev. Dr. Reusch.
Historia ya Kanisa, cha Canon H. J. E. Butcher.
Islam na Uhuru wa watumwa, cha Hadhrat Mirza Bashir Ahmad, M.A.

Vitabu vya Tasawwuf na 'Aqaaid

Tadhkiratul-Auliya, cha Fariid-ud-Din 'Attaar.
Khasaaisul-Kubra.
Al Insaanul-Kaamil, cha Seyid Abdul Karim Jilani.
Maudhu'at Kabir, cha Mullah Ali al-Qari.
Futuuhat Makkiyya, cha Muhyid-Din Ibni Arabi.
'Awaariful Ma'aarif, cha Abu Hafs Umar bin Muhammad.
Dawud Zaahiri.

Malaikat Allah, cha Hadhrat Mirza Bashir-ud-Din Mahmud Ahmad (Khalifatu-Masih II).
Tahdhiirun-Naas, cha Maulana Muhammad Qasim Nanutwi, India.
Uislamu Sahihi, cha Hadhrat Mirza Bashiru-ud-Din Mahamud Ahmad (Khalifatu-Masih II).

Vitabu vya Seyyidna Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad, Masihi Aliyeahidiwa a.s

Haqiiqatul-Wahyi.
Shahaadatul-Qur'an.
Chashma'i Ma'rifat.
Durri Thamin.
Uislam na Hekima yake.
Safina ya Nuhu.
Minanur-Rahmaan.

Vitabu Vingine

Subulus-Salaam.
Ta'rifaat.
Paganism in our Christianity, by Weigal.
The Documents of the Hextateuch, by W.E. Addis, M.A. of Balilol College, Oxford.
Modern Study of the Old Testment and Inspiration, by T.H. Sprott, M.A. Welington, New Zealand.
Shifaa Kadhi 'Ayaadh.
Robertson's Pagan Christs.
Life of Christ by Dean Farrar.
Our son God.
Diodorus Siculus (Translation by C. M. Oldfather, London, 1935).
Book of Common Prayer.
Katekisimu ya Katoliki, Catholic Bookshop, Nairobi.
Biblia: Maagano ya Kale na Mapya ya kila namna: ya wakatoliki na Waprotestanti.
The Sources of Christianity, by Al-Hajj Khwaja Kamalud-Din.
Where did Jesus Die? Cha Maulana Jalal-ud-Din Shams H.A., London.

MPANGO WA TAFSIRI HII

Kabla hujaingia kuisoma Tafsiri hii ingefaa uelewe maelezo haya machache yakuambiayo namna ilivyopangwa Tafsiri hii.

(1) Kila sura imeandikwa kwa jina lake la Kiarabu kwa herufi za Kizungu, na kadhalika kila juzu. Neno FUNGU limetumiwa badala ya neno RUKUU na MAKRA au KARA.

(2) Ukurasa wo wote utakaofungua utakuta juu kabisa jina la sura na nambari yake na kadhalika jina la juzu na nambari yake. Hivyo po pote utakapofunua utajua mara moja kuwa umefunua sura gani, na juzu gani, na aya ya ngapi.

(3) Upande wa kulia ni Qur'an yenyewe kwa Kiarabu, na upande wa kushoto ni tafsiri yake kwa Kiswahili. Herufi zilizoandikwa tafsiri ni kubwa kuliko herufi zilizoandikwa maelezo yake. Maneno ambayo yametiwa katika vifungo vya namna hii:- ( ) katika tafsiri, hayako katika Kiarabu, nayo yameongezwa ili kufafanua maana.

(4) Kunapokuwa aya inayoelezwa, mstari umepigwa kuitenga tafsiri na maelezo. Maelezo yako katika herufi ndogo kuliko tafsiri, na yameandikwa kwa mistari mirefu inayoanza mwanzo wa ukurasa mpaka mwisho.

(5) Si aya zote zilizoandikiwa maelezo. Lakini aya yo yote iliyoandikiwa maelezo, maelezo yake yanaanza na nambari ya aya yenyewe. Kwa mfano, kama aya ya pili au ya kumi ndiyo inayoelezwa, basi utaona chini ya mstari neno **Aya 2** au **Aya 10** katika wino mweusi zaidi, katika ukurasa ule ule wenye aya inayoelezwa. Pengine maelezo hayo huendelea kumalizikia ukurasa ufuatao, mmoja au zaidi.

(6) Unapokuta marejeo yameandikwa, kwa mfano, (sura 3:6) maana yake ni sura ya 3 ya Qur'an na aya ya 6. Ukitazama katika faharisi, utaona sura ya 3 ni Aali Imraan, nayo iko ukurasa wa 92. Pengine hutakuwa na haja ya kuangalia faharisi, bali utafuata tu mfuatano wa nambari za sura juu kabisa ya kurasa mpaka kufikia nambari ya sura uitakayo. Kila mara kumbuka ya kuwa nambari iliyoko upande wa kushoto wa nukta hizi mbili (:) ndiyo nambari ya sura; na iliyoko upande wa kulia ndiyo nambari ya aya.

(7) Kama marejeo ni ya Biblia, basi jina la kitabu maalum cha Biblia litatajwa, kisha nambari za sura za aya zitaandikwa kama ilivyolezwa katika kifungu (6) hapa juu. Kwa mfano, Marko 2:5 maana yake ni kitabu cha Marko, mlango au sura ya pili aya ya tano. Ama ikiandikwa, 2 Wakor. 2:3 maana yake ni kitabu cha pili cha Wakorintho, sura au mlango wa 2 aya ya 3.

Tunapokuwa tumechukuwa marejeo katika Injili ya Wakatoliki, tunaandika majina ya vitabu vya Injili kama wanavyoyaandika wao, kama Mathayo, Marko, Luka, Yohana. Na kama ni marejeo toka Injili za Waprotestani, tunaandika kama desturi, hivi: Matt. (kifupi cha Mattayo au Mathayo, Marko, Luka na Yohana.

(8) Ikiwa nambari inaonyesha ukurasa, basi itaandikwa, kwa mfano, ama ukurasa 20, au kwa kifupi uk. 20 Neno taz. ni kifupisho cha tazama, na n.k.w ni kifupisho cha kadha wa kadha. Neno n.k ni kifupi cha na kadhalika.

(9) Tulifanya kila bidii ili makosa ya chapa, iwezekanavyo, yasitokee. Hivyo, katika uandishi wa Kiswahili makosa ya mashine hakuna yenye maana. Katika hati ya Kiarabu makosa machache ya mashine yamepenya. Lakini wasomao Qur'an mara kwa mara hawatatatizwa. Na pia mahali pachache unaweza kuona dhammah zimekatika mikia, au fat'ha na irabu nyingine zimepata ajali kama hiyo, na kadhalika nukta mojawapo ya nun au fe n.k. Hayo yote ni makosa ya uchapaji yaliyokiuka juhudi yetu, si vigumu kwako kusahihisha. Upungufu wa namna hii unapatikana karibu katika masahafu nyingi zilizopigwa chapa, nao kwa desturi hauwatatizi waliofunzwa vizuri kuisoma Qur'an. Kwa neno zima chapa yenyewe ni nzuri sana.

(10) Jambo la kukumbuka wakati wa kusoma Tafsiri hii ni kwamba, aya za Qur'an zimeandikwa mbalimbali kwa ajili ya anayetaka kujifunza Kiarabu chake, lakini husomwa kwa namna ile ile mtu anavyosoma maandiko mengine. Aya zote zinaungana katika kueleza habari zinazozieleza, zikitiliwa vituo vile vile wanavyotumia watu wote katika maandiko ya herufi za Kizungu. Pengine aya inafika mwisho hali habari inayoieleza haijakatika, bali yaendelea katika Aya moja au zaidi zifuatazo. Hivyo, kwa kuzielewa vizuri, soma kwa kufuata vituo tulivyotia ambavyo ni maarufu katika maandiko yote wanayotumia watu siku hizi.

FAHARISI

Sura		Ukurasa
DIBAJI		v.
MAJINA YA VITABU		viii.
MPANGO WA TAFSIRI		xiii.
FAHARISI		xv.
UTANGULIZI		xvii.
1.	AL-FAATIHA	1
	Juzu 1, Alif Laam Miim	6
2.	AL-BAQARA	6
	Juzu 2, Sayaquulu	40
	Juzu 3, Tilkar-Rusulu	78
3.	AALI 'IMRAAN	93
	Juzu 4, Lan tanaalu	119
4.	AN-NISAA	144
	Juzu 5, Wal muhsanaat	153
	Juzu 6, Laa yuhibbulaahu	183
5.	AL-MAAIDA	199
	Juzu 7, Waidhaa sami'uu	224
6.	AL-AN'AAM	238
	Juzu 8, Walau annanaa	261
7.	AL-A'RAAF	274
	Juzu 9, Qaalal malau	291
8.	AL-ANFAAL	317
	Juzu 10, Wa'lamuu	325
9.	AT-TAUBA	333
	Juzu 11, Ya'tadhiruuna	358
10.	YUUNUS	366
11.	HUUD	399
	Juzu 12, Wamaa min daabbatin	400
12.	YUUSUF	428
	Juzu 13, Wamaa ubarriu	437
13.	AR-RA'D	450
14.	IBRAHIIM	464
15.	AL-HIJR	477
	Juzu 14, Rubamaa	478
16.	AN-NAHL	488
	Juzu 15, Subhaanal-ladhii	510
17.	BANII ISRAAIIL	510
18.	AL-KAHF	529
	Juzu 16, Qaala alam	547
19.	MARYAM	555
20.	TWAA HAA	567
	Juzu 17, Iqtaraba	584
21.	AL-ANBIYAA	584
22.	AL-HAJJ	598
	Juzu 18, Qad aflaha	616
23.	AL-MU'MINUUN	616
24.	AN-NUUR	629
25.	AL-FURQAAN	647
	Juzu 19, Waqaalalladhiina	649
26.	ASH-SHU'ARAA	657
27.	AN-NAML	674
	Juzu 20, Amman khalaqa	682
28.	AL-QASAS	687
29.	AL-'ANKABUUT	701
	Juzu 21, Utlu maa uuhiya	707
30.	AR-RUUM	713
31.	LUQMAAN	723
32.	AS-SAJDA	729
33.	AL-AHZAAB	734
	Juzu 22, Waman yaqnut	741
34.	AS-SABAA	754
35.	AL-FAATIR	763
36.	YAA SIIN	772
	Juzu 23, Wamaa liya	774
37.	AS-SAAFFAAT	781
38.	SAAD	795
39.	AZ-ZUMAR	805
	Juzu 24, Faman adhlam	810
40.	AL-MU'MIN	817
41.	HAA MIIM	829
	Juzu 25, Ilaihi yuraddu	836
42.	ASH-SHUURAA	838
43.	AZ-ZUKHRUF	847
44.	AD-DUKHAAN	856
45.	AL-JAATHIYA	861
	Juzu 26, Haa Miim	867
46.	AL-AHQAAF	867

Sura	*Ukurasa*
47. MUHAMMAD	874
48. AL-FAT'H	881
49. AL-HUJRAAT	888
50. QAAF	892
51. ADH-DHAARIYAAT	896
Juzu 27, Qaala famaa khatbukum	898
52. AT-TUUR	901
53. AN-NAJM	906
54. AL-QAMAR	911
55. AR-RAHMAAN	916
56. AL-WAAQI'A	922
57. AL-HADIID	928
Juzu 28, Qad Sami'al-Laahu	934
58. AL-MUJAADILA	934
59. AL-HASHR	939
60. AL-MUMTAHANA	944
61. AS-SAF	948
62. AL-JUMU'A	951
63. AL-MUNAAFIQUUN	954
64. AT-TAGHAABUN	957
65. AT-TALAAQ	960
66. AT-TAHRIIM	964
Juzu 29, Tabaarakal-ladhii	968
67. AL-MULK	968
68. AL-QALAM	972
69. AL-HAAQQA	977
70. AL-MA'AARIJ	981
71. NUUH	984
72. AL-JINN	987
73. AL-MUZZAMMIL	991
74. AL-MUDDATHTHIR	994
75. AL-QIYAAMA	998
76. AD-DAHR	1002
77. AL-MURSALAAT	1006

Sura	*Ukurasa*
Juzu 30, 'Amma	1010
78. AN-NABA'	1010
79. AN-NAAZI'AAT	1014
80. 'ABASA	1018
81. AT-TAKWIR	1021
82. AL-INFITAAR	1024
83. AL-MUTAFFIFIIN	1026
84. AL-INSHIQAAQ	1029
85. AL-BURUUJ	1031
86. AT-TAARIQ	1034
87. AL-A'LAA	1036
88. AL-GHAASHIYA	1038
89. AL-FAJR	1040
90. AL-BALAD	1043
91. ASH-SHAMS	1045
92. AL-LAIL	1047
93. ADH-DHUHAA	1049
94. ALAM NASHRAH	1051
95. AT-TIIN	1052
96. AL-'ALAQ	1057
97. AL-QADR	1059
98. AL-BAYYINA	1060
99. AZ-ZILZAAL	1062
100. AL-'AADIYAAT	1063
101. AL-QAARI'A	1065
102. AT-TAKAATHUR	1066
103. AL-'ASR	1067
104. AL-HUMAZA	1068
105. AL-FIIL	1069
106. AL-QURAISH	1070
107. AL-MAA-'UUN	1071
108. AL-KAUTHAR	1072
109. AL-KAAFIRUUN	1073
110. AN-NASR	1074
111. AL-LAHAB	1075
112. AL-IKHLAAS	1076
113. AL-FALAQ	1077
114. AN-NAAS	1078



UTANGULIZI

Shukurani hasa ni kwa Allah ambaye kwa msaada Wake mkuu tumepata uwezo na maarifa ya kutimiza kazi ya kuitafsiri Qur'an Tukufu pamoja na kuandika maelezo machache katika lugha ya Kiswahili.

MSAADA MKUU WA ALLAH.

Tuna yakini ya kuwa kazi hii ngumu sana tusingeweza kuimaliza wala tusingewahi kuiweka mbele ya ndugu zetu wapenzi watamkao Kiswahili kwa sura hii kama tusingeongozwa na Allah tangu mwanzo mpaka mwisho wa kazi yenyewe. Kwa hakika mambo mengi na mashaka mengi na upungufu wa namna mbalimbali ulitokea mara kwa mara hata ikafahamika ya kuwa kazi hii haitamalizika, nasi tutaanguka njiani. Lakini Allah, kwa baraka Zake akatuzidishia nguvu na uwezo, na akatuneemesha kwa fadhili zisizo na hesabu, hata taabu ikaondoka, na mashaka yakakatika, na safari tuliyoianza miaka kumi na sita kabla ya leo sasa tumeimaliza, na tumefika salama kwenye makusudio yetu. Alhamdulillahi washshukru-lillahi aliyetuongoza na kutufikisha kwa amani.

HISTORIA YA KAZI YA TAFSIRI

Nakumbuka sana ilikuwa siku ya kwanza ya mwezi Mtukufu wa Ramadhani, siku ya Jumatatu, tarehe 15 Novemba, 1936, baada ya sala ya asubuhi nilipoanza kuandika tafsiri ya Qur'an, mahali paitwapo Minazini katika mji wa Tabora. Niliposhika kazi hii nilikuwa peke yangu, na hakuwepo Mwafrika ye yote wa kunisaidia isipokuwa Mwalimu Sudi Kambi ambaye zamani alikuwa mwalimu wa Ahmadiyya Muslim School Tabora; lakini yeye hakuwa anajua Kiarabu. Baadaye yeye aliondoka Tabora, nami nikaendelea na kazi yangu ya kuandika tafsiri hii. Siku baada ya siku, na wiki baada ya wiki, hata mwaka baada ya mwaka ukapita na kazi ikaendelea, na sehemu kubwa ikamalizika, toka mwanzo mpaka mwisho wa juzu ya thelathini.

Tafsiri ilipigwa taipu, na katika mwisho wa mwaka 1942 au mwanzo wa mwaka 1943 ikapelekwa kwenye idara ya Inter-territorial Languages Committee, na Idara ikapeleka muswada wa tafsiri kwa wasomaji na wachunguzi wa lugha, ili waisome kwa uangalifu na watoe maoni yao juu ya lugha ya tafsiri.

Katika mwaka 1944 mwezi wa Aprili tukapata barua ya Katibu wa Idara hiyo pamoja na maoni ya wasomaji ambao waliandika, "Kwa hali ya jumla, tafsiri ni nzuri sana" isipokuwa yanatakiwa mabadilisho kadha. Mahali pengine tulikubali maoni yao, na pengine hatukuyakubali kwa sababu zinazohusiana na lugha ya Kiarabu.

Hatukuishia hapo, bali nikawapa baadhi ya Waafrika wengine waisome tafsiri hii na watazame hasa lugha. Baadaye ndugu yetu Bwana Kaluta Amri Abedi, kwa kukaa pamoja nasi, akafunzwa na kupata maarifa ya elimu za Qur'an na Kiarabu pia. Yeye akaanza kuichunguza tafsiri hii na kuilinganisha na kuisahihisha. Baada ya muda wakaingia katika kazi hii masheikh wetu wengine

ambao ni wanachuoni wa elimu za Qur'an na za Kiislamu, na pia wenye maarifa ya lugha ya Kiswahili. Wao waliisoma tafsiri hii kwa kuitafakari sana na wakatoa maoni yao. Hawa wote - Waafrika wenye busara na masheikh wetu wataalamu - wakapendezwa na Kiswahili cha maandishi fasihi ya tafsiri hii.

MAELEZO YANAHUSU MAMBO MATATU

Tulipofika hapa ilifikiriwa ya kuwa itakuwa vizuri kama maelezo pia yaandikwe. Mwisho wa mwaka 1949 tukaingia kuandika maelezo yenye shabaha tatu tulizoweka mbele yetu:-

Kwanza. Upinzani unaoletwa na wasiokuwa Waislamu, hasa Wakristo, katika nchi ya Afrika Mashariki katika magazeti yao na vitabu vyao juu ya aya fulani za Qur'an na juu ya maisha ya Mtume Muhammad s.a.w., au juu ya mafundisho ya Kiislamu, upinzani wa namna hii lazima ujibiwe.

Pili. Kwa kulinganisha na mafundisho ya dini nyinginezo ubora wa mafundisho ya Kiislamu uhakikishwe.

Tatu. Makosa yaliyoingia katika Waislamu kwa sababu ya kutojua maneno ya Qur'an, yabainishwe, na haki idhihirike.

Kwa kuandika maelezo, ingawa tumevisoma vitabu vingi na vingine tumevirejea, lakini maelezo mengi kwa hakika tumechukuwa katika tafsiri zilizoandikwa na Hadhrat Mirza Bashir-ud-Din Mahmud Ahmad, ambaye kwa sababu ya utawa na wema wake na kuzama kwake katika huba ya Qur'an Tukufu ameandika tafsiri nzuri kabisa kwa kuchukuzana na haja za Waislamu wa siku hizi. Yatakaposomwa maelezo haya itajulikana ya kuwa Qur'an Tukufu ndicho Kitabu kinachowatimizia wanadamu haja zao katika maendeleo ya kila namna na kinachoweza kuwaongoza sawasawa. Na hata sasa Kitabu hiki kitukufu kina nguvu ya ajabu ya kuwaongoza na kuwainua watu kwenye vilele vya utakatifu na ustawi. Maelezo mengine yameandikwa nami na pia baadhi ya masheikh wetu.

KANUNI YA KUTAFSIRI

Katika tafsiri tumefanya bidii ya kuwa tujue walivyotafsiri wanazuoni wa zamani na wa sasa. Lakini badala ya kuwapendelea wanazuoni fulani na kuwaacha wengine, sisi tulishika njia ya salama kwa kuandika tafsiri inayopatana na aya zingine za Qur'an, na inayopatana na kauli za Mtume s.a.w., na inayokubaliwa na kanuni za lugha ya Kiarabu. Tuna hakika ya kuwa ndugu zetu Waafrika watakapoisoma tafsiri hii watajionea wenyewe ya kuwa tunavyosema hapa juu ni haki. Njia tuliyoshika kwa kutoa tafsiri ndiyo njia kubwa ya kupata maarifa hasa ya Qur'an pamoja na utakaso wa moyo na usafi wa roho.

Katika kutafsiri tumejaribu sana ya kuwa tuandike tafsiri ya neno kwa neno, na pia tusiharibu ladha na utamu na ufasihi wa lugha ya Kiswahili, na kadhalika lugha isiwe ngumu sana. Wasomaji wataona wenyewe jinsi tulivyoshinda katika jaribio hili.

Zamani Padre Godfrey Dale aliandika tafsiri ya Qur'an. Lakini kwa sababu yeye hakuwa na maarifa ya Kiarabu alishindwa mahali pengi kuandika tafsiri iliyo sawa. Mara nyingi hakufahamu neno la Kiarabu, na alichukua toka tafsiri ya Kiingereza baadhi ya maneno na

kuyageuza kwa Kiswahili bila kupeleleza maneno ya asili. Zaidi ya hayo kusudi lote la tafsiri yake ni kuipinga na kuikashifu dini ya Kiislamu. Hivyo tafsiri ya Padre Dale ina uharibifu mwingi unaotokana na kutojua kwake, na kadhalika unaotokana na uadui wake uliopitiliza mipaka.

Kadhalika katika tafsiri yake, Padre Dale, hakuandika maneno ya asili ya Kiarabu ili watu wangepata kujua amekosa wapi, na amekosa nini au amezidisha nini na kupunguza nini.

QUR'AN NI NENO HALISI LA MUNGU

Katika tafsiri hii tunayoweka mbele yenu tumeipiga chapa Qur'an Tukufu kwa Kiarabu pia, na kila aya imewekwa katika sehemu mbali na nyingine ili watu wajue tafsiri ya maneno ya Kiarabu vizuri zaidi. Kadhalika tumezitilia nambari aya zote toka Bismillahi, katika Kiarabu na Kiswahili, ili iwe rahisi kwa ajili ya marejeo. Kwa hakika kupiga chapa tafsiri ya Qur'an bila kuweka Kiarabu kuna hatari kubwa ya kupotea makusudio hasa ya maneno ya asili, jinsi tuonavyo katika Biblia maneno yake ya asili yalivyopotea, na kwa kuchapa tafsiri tu maneno yanaendelea kubadilika mara kwa mara. Lakini kama kungekuwako maneno ya asili, watu wangejua na kutambua sahihi ni nini.

Sasa Waafrika kwa rehema za Allah wanaendelea mbele, nao wana haja ya kupata maarifa ya juu na maoni ya haki. Leo katika ulimwengu hakuna kitabu cha maarifa hasa, wala hakuna maneno ya Allah yanayopatikana katika hali ya asili isipokuwa katika Qur'an Tukufu. Maneno yanayopatikana katika Qur'an Tukufu toka mwanzo mpaka mwisho ni ya Allah Mwenyewe tu, hakuna mchanganyiko wa maneno ya watu na ya Mungu ndani yake; bali ni ufunuo na wahyi safi wa Allah uliomo katika Qur'an. Kwa hiyo juu ya uso wa ardhi na chini ya mbingu kama kitabu cho chote kinaweza kustahili kuitwa Kitabu Kitakatifu cha Mungu ni Qur'an Tukufu tu. Na kama kuna maneno yo yote yanayoweza kuitwa maneno ya Mungu ni maneno ya Qur'an Tukufu tu. Haya ndiyo maneno yaliyolindwa na Allah tangu kuteremshwa, na Allah akayawekea ahadi ya kuyalinda daima kama ionekanavyo katika sura 15:10. Hiyo ndiyo hakika ambayo hata maadui wa Uislamu wameikubali ya kuwa kweli Qur'an iko katika hali ile ile iliyokuwa nayo wakati ilipoteremshwa kwa Mtume Muhammad s.a.w., bila neno moja kuzidishwa au kupunguzwa. Allah ndiye Mtakatifu naye ndiye aliyesema haki.

Maadamu Qur'an ni Neno la Mungu, tena Neno halisi, na Mungu ndiye Mwumba wa ulimwengu na Mjuzi wa haja za watu Wake, basi anaweza kuwaongoza kwa Maneno Yake; na Maneno Yake tu ndiyo yanayoweza kuwafikisha wayafuatao kwenye vyeo vikubwa. Nina yakini Waafrika jinsi wanavyoonekana katika taabu za namna mbalimbali katika nchi mbalimbali, wao wana haja ya mwongozo, na mwongozo mwingine hakuna isipokuwa mwongozo wa Qur'an Tukufu.

NI LAZIMA KUPATA MAARIFA YA QUR'AN

Waislamu katika nchi hii pia wako katika hali ya unyonge na ya chini sana. Na sababu yake kubwa ni kwamba wao pia hawana maarifa ya Qur'an Tukufu. Bila shaka wanajua kuisoma Qur'an, hata pengine kwa tajwidi na kwa sauti nzuri. Lakini wangapi wanaojua ya kuwa Mola

wao na Mwumba wao anawataka nini? Qur'an Tukufu iko katika Kiarabu, na wasiofahamu Kiarabu hawajui sawasawa matlabu na maana ya Qur'an. Na bila kujua maneno ya maarifa na hekima watawezaje kuyafuata? Basi kujua na kupata elimu ni jambo kubwa, tena la kwanza. Hivyo Waislamu watajua pia tafsiri ya maneno ya Kiarabu walichokuwa wanakisoma tangu zamani; na zaidi ya hayo Waislamu baada ya kupata elimu na maarifa ya Qur'an kwa kusoma tafsiri, bila shaka watapata uimara kabisa katika imani yao, na wataona fahari ya kujua ilivyo heshima yao mbele ya Allah kwa sababu ya kushika kwao dini ya Kiislamu na kufuata mafundisho ya Qur'an.

UZIMA WA MATAIFA UMO KATIKA QUR'AN

Basi uzima wa Waislamu na kuinuka kwa Waafrika, la, bali uzima wa mataifa yote umo katika kushika mafundisho ya Qur'an Tukufu.

Katika pande zote za dunia - Ulaya na Amerika, Asia na Afrika - watu wameanza kusema ya kuwa Ukristo hauwafai watu katika maendeleo na tabia za kiroho na katika ustawi wa kidunia. Si haya tu bali wanaacha mafundisho ya Ukristo na bila kuwa na habari wanaanza kufuata baadhi ya mafundisho bora ya Qur'an na ya Mtume wetu Muhammad s.a.w. Afrika ya mashariki na ya kati sasa karibu kuingia katika boma la Qur'an Tukufu na kupata amani katika ngome ya Uislamu! Sasa ni kazi yenu, enyi ndugu zangu Waislamu, kuweka mbele yao Kitabu hiki Kitukufu kilichoelezwa kwa lugha yenu nzuri na tamu ya Kiswahili, ili ninyi na wao nyote mpate faida ya mwili na roho na msalimike na mwokoke. "Qur'an Tukufu ndiyo iliyofungua njia za wokovu wa kweli na uliokamilika; na baki yote ni vivuli vyake. Someni Qur'an kwa kuitafakari na ipendeni sana, kuipenda ambako hamjakipenda cho chote, maana heri zote zimo katika Qur'an tu.

"Hakika Qur'an ni chemchem ya kufaulu kwenu na kuokoka kwenu. Minghairi ya Qur'an Tukufu hapana Kitabu kingine chini ya mbingu kinachoweza kuwaongozeni. Allah amewafanyieni hisani kubwa kuwapeni Kitabu kama Qur'an Tukufu. Kwa hiyo msiache Qur'an Tukufu ovyo, kwani katika Qur'an Tukufu tu ndimo umo uzima wenu. Watakaokiheshimu watapata heshima mbinguni, na watakaoitanguliza Qur'an Tukufu kuliko hadithi zote na maneno yote wao watatangulizwa mbinguni. Sikilizeni! na sasa hakuna kitabu cho chote kitakachoweza kumwongoza mwanadamu juu ya ardhi ila Qur'an Tukufu; na hakuna Mtume wala mwombezi mwingine wa wanadamu ila Mtume Muhammad s.a.w. Jitahidini mumpende kwa mapenzi kweli kweli Mtume huyu - Mtume wa heshima na utukufu; wala msimheshimu mtu ye yote kuliko yeye ili mwandikwe mbinguni pamoja na waliookoka." (Safina ya Nuhu).

SHUKURANI KWA WALIOSAIDIA

Sasa inabidi niwatajieni, kwa kutoa shukurani, wenzangu waliofanya kazi hii pamoja nami katika miaka hii miwili mitatu kwa juhudi kubwa na kwa shauku nyingi, hasa mpenzi ndugu K. Amri Abedi Kaluta wa Ujiji, na Maulana Muhammad Munawwar. Kwa hakika wenzangu hawa wawili pamoja nami walishughulika sana katika kuisoma tafsiri na kuandika maelezo na kusahihisha *proofs (Miswada)* na kazi nyingine nyingi zinazohusiana na tafsiri hii.

Maulana Inayat Ullah Khalil pia alinisaidia kwa kutafuta maneno mbalimbali katika Hadithi

za Mtume s.a.w. na katika vitabu vya tafsiri. Sheikh Jalal-ud-Din Qamar, kwa kuandika maelezo machache na kusahihisha (miswada) *proofs* za mwisho za Kiarabu na Kiswahili, pia amenisaidia.

Waidha namshukuru sana Hadhrat Amir-ul-Muuminiin Khalifat-ul-Masih II Hadhrat Mirza Bashir-ud-Din Mahmud Ahmad r.a., Kiongozi Mkuu wa Jumuiya ya Waislamu wa Ahmadiyya , kwa kuniruhusu kutumia miswada ya hati ya Kiarabu ambayo niliiazima kwake na kuileta inakiliwe na kutiwa katika tafsiri hii. Pia namshukuru kwa kutuandikia Dibaji ya Tafsiri hii ambayo nilimwomba aiandike.

Pia nawashukuru ndugu zangu na rafiki zangu waliotoa michango ya maelfu ya shilingi kwa ajili ya kazi hii ambao sikuwataja hapa kwa sababu hawakutaka majina yao yatajwe. Hawa wote tunawaombea rehema na mafanikio katika dunia na Akhera.

Mwishoni ninawaomba ndugu zangu watakapoisoma tafsiri hii kama wataona kosa lo lote watuletee habari, wala wasikae kimya, maana sisi ni wanadamu tu na tumefanya bidii kutengeneza tafsiri hii iwe nzuri kwa kila hali. Juu ya hayo mnajua sana ya kuwa asiye na kosa ni Allah tu. Tutakuwa na furaha kujaribu kusahihisha katika chapa ya pili kama kutakuwa na kosa la kweli. Na ama wale watakaopata kujua ya kuwa kazi hii ni yenye manufaa kweli kwa watu, basi watuombee heri kwa Allah katika dunia na Akhera. Mola wetu awe radhi nasi, nasi tuwe radhi naye - Amin.

MAOMBI KWA ALLAH

Mwisho wa yote haya naelekea Kwako, Ee Mola wangu na Mwumba wangu, uliyewapa ndugu zangu na rafiki zangu nia ya kutoa msaada wa elimu na fahamu na fedha ili kuitimiza kazi hii kwa namna nzuri, uwape malipo mema katika dunia na Akhera. Na utusamehe makosa yetu, na kwa rehema Zako hasa uifanye Tafsiri hii iwe sababu kubwa ya kuwaongoza watu kwenye dini yako ya Kiislamu na utie baraka katika juhudi yetu hata iwe pia sababu ya kutufikisha kwa hali nzuri katika baraza Lako la utakatifu. Jina Lako la adhama liinuke, na bendera ya Qur'an Tukufu isimikwe - Amin.

Ee Mola wetu, tupokelee, hakika Wewe ndiwe Msikiaji wa maombi; na tuelekee, hakika Wewe ndiwe Mpokeaji wa toba na Mrehemevu.

Na neno langu la mwisho ni kwamba Sifa zote njema zinamhusu Allah, Mola wa walimwengu.

SHEIKH MUBARAK AHMAD
Mbashiri wa Islam

Ahmadiyya Mosque
Nairobi,
11th March, 1953.
25th Jamad Thani 1372 Hijriyya.
11th Aman 1332 Shamsi Hijriyya.

FAHARISI

Ya mambo yaliyotajwa katika Qur'an na Tafsiri

HAPA chini mtasoma faharisi ya baadhi ya mambo yaliyoelezwa katika tafsiri yetu ya Qur'an Tukufu au yaliyopata kutajwa katika aya zake. Tafsiri hii ilitolewa mnamo mwaka 1953 na tangu wakati huo tulikuwa na hamu ya kutengeneza faharisi kama hii ili wasomaji wake waweze kutafuta kwa urahisi jambo walilohitaji kulifahamu mara moja.

Ni rahisi kutumia Faharisi hii. Tumeweka namba mbili tu. Ya kwanza ni ukurasa wa Tafsiri yetu na ya pili ya Qur'an. Kwa mfano, 299/158 maana yake ni ukurasa 299 wa Tafsiri yetu na aya iliyoelezwa kwenye ukurasa huo ni ya 158. Ukifunua hapo utasoma baadhi ya bishara za Biblia zinazotabiri ufikaji wa Mtume Muhammad, amani na rehema za Allah ziwe kwake. Kwa kuwa maelezo hayo yanaendelea mpaka ukurasa 304, tumeandika hivi "299-304/158". Habari hii mtaikuta chini ya "Biblia" na "Muhammad". Uharamu wa nyama ya nguruwe mtasoma chini ya "Nguruwe" katika 48-50/174. Hasara za pombe mtasoma chini ya "Ulevi" katika 65-67/220 na kadhalika. Ni afadhali sana mtalii mara moja Faharisi hii yote tangu mwanzo hadi mwisho mpate kuelewa mpango wake.

Faharisi hii imepangwa na Sheikh Muhammad Munawwar. Shukrani hasa ni kwa Allah Aliyemwezesha kuikamilisha kazi hii ya maana sana. Mungu Ampe uwezo zaidi wa kuitumikia Qur'an. *Amin.*

Adamu:
si mtu wa kwanza duniani 13,14/31; 275 - 277/12
malaika kumtii 14,15/35
hakuwekwa peponi 15/36; 279/25
hakuwa na nia ya kuasi 277, 278/21
kupotezwa na Iblisi 275 - 277/12
alitambua udhaifu wake 278/23
ametajwa katika "Tin" 1052/2
habari ya wanawe wawili 208, 209/28-32

Adhabu:
ya duniani 23/66; 24/67; 462/40; 706,707/41; 819/19; 1013/41;
kwa wahalifu 209/34
kwa wezi 210, 211/39
kwa makafiri 247/46; 323/33
kwa viongozi wa makafiri 264/124
watu wa Makka kuonywa 292/98
si ya kishenzi 319, 320/13
ya duniani huja kwa kuizuia haki 601/18
inaweza kuahirishwa au kuondolewa 383, 384/47; 407, 408/34
ya Mungu ni kali sana 452/7
fidia haikubaliwi 456/19
huteremka baada ya watu kuonywa 513/16; 1013/41
wenye kuadhibiwa wasihurumiwe 629, 630/3
ishara za adhabu pia zipo 709/51
zipo hata siku hizi 709, 710/56
shabaha yake 732/22
ya kukosa kupata ulichotamani 762/55
itakuja ghafla 777/51
ingeshuka upesi, lakini 838/6
ya njaa 857/11; 970/22
ya akhera kwa makafiri 522/73; 931/21
njia ya kuiepuka 984/4
iwe sawa na ubaya 509/127

Ad-dhikr:
maana yake 494/45; 585/11

Ahadi:
itekelezwe 50, 51/178; 199/2; 457/21; 516/35; 616/9; 983/33
ya Mungu itimizwe 271/153; 502/92
za Mtume zitatimia 1006/8
laana kwa wavunjaji ahadi 204, 205/14-15

Akhera:
waaminio watatunzwa 12/26; 475/46; 1001/24
juhudi itakubaliwa 513/20
kila kitendo kina malipo 540/50; 569/16
adhabu ya Akhera ni kubwa 809/27; 1032/13
wenye kuikataa wataadhibiwa 512/11
fikara za wenye kuikataa zakanushwa 243/30; 493, 494/39-41; 518/50-52; 780/78-83;

Amri ya Mungu:
maana yake 488/2; 492/34

Ardhi:
ni makazi kwa watu 279/26; 1007/26, 27
na mbingu viliumbwa katika miaka
maelfu 284/55; 367-369/4
ina wasaa 807/11
itatoa mizigo 1062/3

Ayubu:
Habari zake 194/164; 254/85; 593/84, 85 800, 801/42-45

Baha'i:
wanaficha vitabu vya Bab na Bahaullah 406/26

Bahiira:
maana yake 229/104

Biblia:
Ahadi ya Biblia imetimia 3/1
imegeuzwa 17-18/43; 204/14; 478, 479/10
haitaji idadi ya chemchem 20, 21/61
imekosea idadi ya Mayahudi 75/244
haina uzuri wa Qur'an 80, 81/256
haina sheria juu ya deni 89, 90/283
imekosea kumtaja Isihaka 789/113
imeleta utumwa 139-142/196
hitilafu ndani yake 165-168/83
inaeleza sawasawa habari ya wachawi 296/124
inamtabiri Mtume 303-308/158; 758, 759/31
haitaji habari ya kusalimika kwa kiwiliwili cha Firauni 394, 395/93
pengine haipatani na Qur'an 430, 431/18

kulinganishwa na Qur'an 478, 479/10
inawasingizia nduguze Yusuf 438, 439/60
na Qur'an vinapatanishwa 443, 444/81
inamsingizia Harun 576, 577/91
inamsingizia Daud 797, 798/24

Bishara:
ya Uislam kuenea sehemu zote 35/116
ya kundi la Mungu kushinda 128/140; 215/57; 938/22
ya kumlinda Mtume 218/68
ina wakati wake 250/68
ya maadui kuangamia 579/106; 983/42; 1046/16
kanuni za bishara za adhabu 407, 408/34
ya kushinda falme na hazina 601/24; 1038, 1039/9-17
ya vitu vipya kutengenezwa 489/9
ikitimia itahakikisha Umoja wa Mungu 528/112
ya kushinda Makka 700/86; 876/14; 1043/3; 1046/16
ya Abu Jahal kuuawa 1058/16
ya farasi kutumiwa na sahaba 1063/2
ya ushindi wa kwanza wa Uislamu 1074/2
ya adui mmoja mkubwa na mkewe kuangamia 1075/2
ya Wakristo waliolala kuamka 533/19
siku moja katika bishara 758, 759/31
ya kupata mateka mengi 885/21
ya kushinda vitani 914, 915/46
ya Qur'an imetimia 917/20; 1021, 1022/2-14; 1024/5
ya njaa 970/22; 1038/2
juu ya adui mwingine 973/17
kuhusu uhamiaji Madina 1036/9
ya ardhi kutoa mizigo 1062/3

Buibui:
nyumba yake 707/42

Bustani:
mfano wake 537/35

Chakula:
namna zake 47/169; 225/88; 225/89
kilichoharimishwa 48-50/174; 269/146
uwindaji umeruhusiwa 201/5
kwenye watu wa Kitabu 201, 202/6
uchaji pia katika kula 226/94
kushika kiasi katika kula 280/32
kuwapa maskini, yatima na mfungwa 1003/9; 1041/18, 19
wanafunzi wa Yesu hawakuteremshiwa toka mbinguni 232, 233/115, 116
Manabii hula 585/9
vyakula safi huzalisha vitendo vizuri 47/169; 622/52
adabu za kukaribishwa 750/54
nyama ni chakula pia 828/80
samaki pia ni chakula 227/97

Dajjal:
maana yake 554/111

Daudi:
mwanaye alimrithi 676/17
alifundishwa kuyeyusha chuma 755/11
amesingiziwa na Biblia 797, 798/24

Dhambi:
tofauti baina ya dhambi na hatia 175/113

Dhul-kifl:
habari zake 593/86

Dhul-Qarnain:
habari zake 551-552/84-99

Falastini:
kukaliwa na wenye haki 596/106, 107

Firauni:
kiwiliwili chake kuhifadhika 394, 395/93
mkewe 967/12, 13

Haami:
maana yake 229/104

Haji:
inakumbusha sadaka ya Hajira na Ismail 45/159
maelezo yake na faida yake 58,59/197; 120/98; 602, 605/27-38
tangazo wakati wa Haji 333, 334/3
miezi ya Haji 59/198
uwindaji umekatazwa 199/2; 227/97
inaleta faida ya kidunia pia 228/98

Mtume kuzuiwa kufanya Haji ndogo 885/19

Harun:
habari zake 299/143; 301, 302/151

Hijr:
maana yake 267/139

Husuda:
pazia yake 518/46
ubaya wake 1077/6

Huud:
habari zake 286, 287/66-73; 412-414/51-61; 871, 872/22-27

Ibada:
maana yake 4/5; 399/3
amri yake 11/22, 23; 273/163-165
ya kushinda msikitini 55,56/188
kwa siri pia 316/206, 207

Iblisi:
hakuwa malaika 14, 15/35
alijivuna 14, 15/35; 275, 276/12, 13; 540/51; 803/75
wafuasi wake watakwenda motoni 277/19; 482/33-45

Ibrahimu:
dua yake 37, 38/127-130; 473, 474/36-38; 474, 475/41, 42
kuhojiana na Nimrodi 82/259
aliyetajwa ni babaake mdogo 252/75; 561/46
Mtume anakurubiana sana naye 114/69
alionyeshwa ufalme wa Mungu 252, 253/76
namna ya mjadala wake 253-254/77-84
habari zake nyingine 416-417/70-76; 474, 475/38-42; 590/52
hakusema uwongo 560/42; 591/64; 787/90
utii wake 788/104
kuomba kwake msamaha 475/42
ameitwa Mwislamu 114/68; 615/79
alikaribisha wageni 897, 898/25-28
hakuwa Myahudi wala Mkristo 114/68

Idi kubwa:
asili yake 788/108

Ilyasa:
kupaa kwake 790/124

Imani:
na vitendo vizuri 12/26
ifuatane na mabadiliko halisi 370/5; 371, 372/10; 392/85; 1032/12; 1067/2-4
na vitendo vifaavyo 1032/12
ya Firauni 392/92
na kumpenda Mungu 405/24
inaleta heshima 407/30
hupatikana kwa hisani ya Mungu 893/18
tofauti ya Islam na Imani 893/15
itikieni wito wake 929/8, 9

Isa bin Maryam:
kasaidiwa na Roho 28/88
Mtume kwa Wayahudi 103-107/50; 647/2
alifundisha umoja wa Mungu 219/73
miujiza yake 103/50; 110-112/60; 519, 520/60
si Mungu 110/60
Mungu alimlinda 231, 232/111
wanafunzi wake hawakuteremshiwa chakula 232, 233/115, 116
amefariki 108, 109/56; 192, 193/160; 236/118; 491/22; 559/32; 559, 560/34; 585/9; 779/69
si mwana wa Mungu 340-344/30
hakufa msalabani 185-190/158; 938/22
hakupaa mbinguni 190-192/159; 1007/26, 27
si hakimu 233, 236/117
alizaliwa bila baba 184/157; 558/21
alizikwa Kashmir 621, 622/51
watu wa pango ni wafuasi wake 530, 531/10
Mtumishi wa Mungu 195, 196/173, 174; 559/31
alisali na kutoa Zaka 559/32
alitukuzwa 640/37; 936, 937/12
alikataa kuonyesha ishara 709/51
hakuumba kitu 7247/12; 867/5
hawi Mungu kwa kuitwa "neno" 727/28

Isihaka:
habari zake 474/40

Islamu:
peke yake ni dini ya kweli 97/20
ni dini ya Manabii wa zamani 118/85; 840/14
dini nyingine haitakubaliwa 118/86
mwongozo kamili umo ndani yake 97/21; 988/15
hakuna dini bora kuliko hii 177/126
haina udhia 54/186; 202/7; 615/79
maana yake ni utii uliokamilika 61/209
hakuna mwenye kuishinda 329/60; 463/42; 523/82; 589/45; 762/50
ni njia iliyonyooka 271/154
inaamrisha kumtii Mtume 99/32; 127/133; 162/65, 66
inaamrisha kutii serikali 160, 161/60
inaamrisha wema kwa wazazi 156/37; 514, 515/24, 25; 702/9; 725/15; 870/16 (wazazi wakiamrisha ukafiri wasitiiwe 702/9; 725/16)
inapendelea wema hata kwa maadui 945, 946/9
inakataza kuwaelekea wadhalimu 425/114
inahimiza kusaidia maskini 897/20; 982/25, 26; 1003/9-11; 1044/15, 17
inasifu kuwapendelea waaminio 941/10
itashinda mara ya pili 22/63; 345/33
inasifu unyenyekevu 604/35; 655/64; 726/19
inafundisha mwendo wa katikati 280/32; 509/127; 515/30; 528/111; 655/68; 726/20
inahimiza kusema maneno mazuri 519/54; 602/25
inafundisha maangalizi ya yatima 63/216; 67/221; 1041/18
inafundisha kumtegemea Mungu 468/13; 654/59; 961/4
inakataza ushirikina 176/117; 514/24; 603/31; 826/65-67
inakataza kuwaoa washirikina 67/222; 946/11
inakataza dhana mbaya 890 /13
inakataza kufuja mali 515/27, 28
inakataza ubahili 157/38; 880/39; 932/25; 941/10; 959/17; 1047/9-11
inakataza kumsogelea mke katika hedhi 68/223
inakataza majivuno 156/37; 932/24
imeleta undugu wa waaminio 889, 890/11
haikuenea kwa upanga 81/257; 396, 397/100; 536/30; 605-609/40; 654/58; 695, 696/ 57; 881/2; 1057/2-6
inakataza uwongo 603/31; 656/73; 814/61; 862/8; 948/3
imeharimisha riba 87, 88/276; 719/40
inakataza hiyana 174/106-108; 819/20
imeleta sheria nzuri kuhusu deni 89, 90/283
imekataza ukataji tamaa 444/88; 483/57; 813/54
imekataza maneno ya upuuzi 616/4; 656/73; 997/46
imeharimisha mambo ya aibu 280/34; 501, 502/91
imegawa urithi 196/177;
imekamilika 200/4
imekataza husuda 160/55; 1077/6
imekataza kuwaua watoto 516/32
uzuri wake 315/200
adhabu zake si za kishenzi 319, 320/13
ina mawazo mapana 382, 383/42
imeweka sheria za kutawala tamaa 549/82
ni dini ya maumbile ya mtu 717, 718/31
inakataza uzinifu 516/33; 629, 630/3; 655/69
imewapa watumwa uhuru 636-639/34; 875/5
vizuizi katika njia yake 773/10
imeleta matokeo mema 775/34
inafundisha njia ya kupatanisha 889, 890/10, 11
inakomesha tofauti za rangi na kabila 890, 891/12-14
inakata mizizi ya ukomyunisti 897/20; 940/8
inakataza mikutano ya siri 936/10
imefundisha usafi 157, 158/44; 202/7; 280/32,33; 603/30; 994/5, 6
inahimiza kuziheshimu alama za Mungu 603/33

inakataza usingiziaji 890/12; 973/11, 12; 1068/2
inafundisha shukrani 724/13
inaamrisha usamehevu 128/135; 633/23
inahimiza kuomba msamaha 128/134, 136, 137; 222/75; 993/21
inakataza kufuata dhana 380/37
inahimiza kutoa mali 128/135; 956/11
inaamrisha subira 17/46; 44, 45/154, 156, 157; 143/201; 457, 458/23; 494/43; 509/128; 604/36; 1044/18
inahimiza uadilifu 202/9; 271/153; 494/91; 932/26
inahimiza kukaribisha wageni 50, 51/178; 515/27; 718/39
inahimiza kulinda tupu 616/6-8; 634/31; 644, 645/61
inahimiza kusaidiana 199, 200/3
inafundisha wema kwa jirani 156/37
inahimiza hisani kwa walio wa chini 156/37
ushindi wake wa kwanza 1074/2
inaeleza haki za ndugu 515/27; 718/39
inaeleza haki ya aombaye na ajizuiaye 897/20
inaeleza haki za watoto 149, 150/12; 498/72; 516/32; 539/47
inaruhusu kuoa wake wanne 144-147/4

Israa:
habari zake 510/2

Jihadi:
ifanywe kwa Qur'an 653/53

Jizya:
maelezo yake 339, 340/29

Kaaba:
kuendewa na watu 37/126
ni Nyumba Tukufu 199, 200/3; 228/98
ni Msikiti Mtukufu 510/2
mumini ni mtakatifu zaidi kuliko 337/19
ni Nyumba inayozuriwa 896/5
kulindwa kwake 1069/2
haiabudiwi 1070/4

Kafara:
kubatilishwa kwake 442, 443/80; 513/16; 897/22; 1024/7; 1052-1056/5

Kamari:
hatari zake 65-67/220
mapadre wanailaumu 226/91

Kanuud:
maana yake 1063, 1064/7

Kauthar:
maana zake 1072/2

Khatamannabiyyin:
maelezo yake 745 - 748/41

Kibla:
kugeuzwa kwake 40, 41/143, 144

Kifo:
maana zake 19/57; 44/155; 775/34
chafanana na usingizi 249/61
ni kitu cha lazima 588/35, 36
hakina kurudi duniani 626/100, 101

Kisasi:
amri yake na fidia yake 51, 52/179, 180
adhabu iwe sawa na ubaya 509/127
vitu vitakatifu vimewekewa kisasi 57/195

Luqman:
mtawa Mhabeshi 723
alitoa mafunzo kama ya Yesu 726/20

Luut:
habari zake 289/81; 418/78-81; 484, 485/63-75; 668, 669/161-174; 681, 682/55-58; 913, 914/34-40
mkewe 669/172; 682/58
hali ya maadui wake 898/33-35
waliomkataa waliwakadhibisha Mitume wote 668/161; 913/34

Maa'uun:
maana yake 1071/8

Madhambi makuu:
maelezo yake 909/33

Majini:
kati ya watu 261/113; 265/129; 265, 266/131; 872/30; 917/14; 987/2
kuumbwa katika moto 481/28
walidhani nabii hatatumwa 988/8

Malaika:
sifa zao na kazi zao 763/2; 818/8-10; 838/6
kumtii Adam 14, 15/35; 275, 276/12; 481/30; 520/62; 580/117
watu watawa kuitwa 31, 32/103; 433, 434/32
walimlinda Mtume 453, 454/12
huleta adhabu kwa makafiri 649/22
mkutano wao 781/9
sio binti za Mungu 792/150; 792/159
huwateremkia waaminio duniani 833/31, 32; 869/14
waaminio wanawaamini 51/178
matokeo ya kuwachukia 30/98, 99
kuwakataa ni upotevu 180/137
hawamwasi Mungu 966/7
hawahesabiki 793/165; 1001/32
nguvu zao zina mipaka 14/33
wanamsalia Mtume 751/57

Mali:
amri ya kuitoa 7/4; 58/196; 929/8, 11, 12; 956/11; 959/16-19
itolewe iliyo nzuri 119/93
itolewe katika dhiki na faraja 128/135
namna ya kuitumia 515/27-30
itolewe hali mioyo inaogopa 623/61
humtilia mtu kiburi 698, 699/77
mwenye kuitoa hapati hasara
itarudi 84/262; 87/273; 929/12
isijikusanye katika mikono ya matajiri 940/8
ya Abubakar ilimsaidia sana Mtume 1048/19
utoaji usifuatwe na udhia na masimbulizi 84, 85/263-265
itolewe kwa siri na dhahiri 86/272; 87/275
ya waaminio ni ya Mungu 362/111

Maryam:
habari zake 101-103/43-48; 557-559/17-30; 594/92
alikula chakula 222/76
alikimbilia Kashmir 621, 622/51
mfano wake 967/12, 13

Masihi Aliyeahidiwa
amefika kwa kuunganisha watu 390, 391/77
ni Shahidi wa ukweli wa mtume 403, 404/18
amehakikisha ubora wa Kiarabu 465/5
wafuasi wake 214, 215/55; 535, 536/29; 887/30; 1031/5
adui zake kuugua tauni 685/83
mfano wa Isa 852/58
kushuka kwake 932/26
Islam itapata ushindi katika wakati wake 949/10
ni Mwajemi 951/4
alama za Akherizamani 1021, 1022/2-14
ni mwezi 1045/3

Mbingu:
mwanzoni ilikuwa gesi 830/12
zilikamilishwa katika duara mbili 830/13
njia za sayari 776/39-42; 896/8
zitapanuliwa 899/48
kutanduliwa 1022/12

Mbwa:
wa mawindo 201/5
hali ya mbwa 312/177

Mgeni:
kumkaribisha 50, 51/178; 515/27; 718/39
namna ya kumkaribisha 897, 898/25-28

Milima:
maana yake 459, 460/32; 579/106; 685, 686/89
kunyanyuliwa 23/64
sura ya Qur'an inaitwa Mlima 901

Miiraji:
maelezo yake 906, 907/2-19
mwujiza huo haukuwatuliza makafiri 525/94
ya Nabii Musa 542-550/61-83

Misikiti:
watu wasizuiwe kuingia 34/115
kujitakasa kabla ya kuingia 280/32
mitukufu miwili imetajwa 510/2
ya wanafiki isisaliwe humo 360, 362/107-110

Miujiza:
ya Nabii Isa 110-112/60
haikataliwi na Qur'an 244, 245/36
ya mtume 569/23; 655/64; 911/2

Mkutano:
wa kufaa 175, 176/115
wa siri 936/10
adabu zake 646/63, 64; 936, 937/12-14

Moto:
ni kama hospitali 319, 320/13
ni wa muda 384/53; 424/109; 1011, 1012/24; 1065/10
wa kidunia 564/72, 73
ni vita pia 10/18; 216/65; 568/11
wakazi wake watawashitaki viongozi wao 753/68
sifa za watu wa motoni 982/18-22; 1034/ 2-5
watu wema hawatauona 595, 596/102-104
si Mungu 675/9
mti wa Jahanamu 785/63; 925/53
vyakula vya watu wa motoni 919/44, 45; 1011, 1012/25-27; 1038/5-8
makafiri watauingia 11/25; 778/64, 65; 810/33; 862/8-11; 997/42-49; 1011/23
watu wa motoni hawataweza kutoroka 731/21
milango yake saba 482/45
walinzi wake 996/31, 32
mlango wake ni kutotumia akili 312, 313/180
mlango wake mmoja ni kiburi 865/32; 984, 985/8
mlango wake mwingine ni tamaa 1002/5; 1004/19; 1066/2
una wasaa 894/31
adhabu kuanza tangu duniani 1016/41
toka mbinguni katika vita 918/36
wa Jahanamu kuokwa 1022/13

Mubahala:
maana yake 112, 113/62

Muhammad s.a.w.:
Ibrahimu aliomba juu yake 38/130
ni mbora wa Mitume 78, 79/254;
hakunukuu toka Injili 84/262
aliteremshiwa fadhili nyingi 175/114
amri ya Mungu ilimtia hofu 425, 426/113
anafanana na Yusuf 428/2; 429/8; 438/59; 439/63; 445/93; 447/104
nguzo za kazi yake hazionekani 450, 451/3
ni tofauti na Waarabu wengine 452/5
alilindwa na malaika 453, 454/12
sahaba zake 207/23; 359/100; 363/117; 640/38; 738, 739/23, 24; 760/40; 885/19; 938/23; 941/10; 1048/19; 1061/9
alilindwa na Mungu 218/68
wa kwanza katika wenye kusilimu 240, 241/15
ni mshindi na mkweli 242/22
hafukuzi maskini na wanyonge 248/53
ishara zilionekana wakati wake 261/112
Mtume kwa dunia nzima 165/80; 266/132; 308, 309/159; 465/5; 597/108; 647/2; 758/29
mwujiza wake 294/108; 463/42; 569/23; 655/64; 911/2
ametuondolea mizigo 303-308/158
kutupa kwake ni kutupa kwa Mungu 320/18
ni Mtumishi wa Mungu 545/66
maadui walitaka kumfunga au kumwua au kumfukuza 322, 323/31; 336/13; 347, 348/40; 876/14
Musa na Isa katika wafuasi wake 233, 236/117; 546/70
kufufua wafu wa kiroho 321/25; 569/21
ni Mtume wa kweli 374, 375/17; 403, 404/18; 449/112
mkono wake mweupe ni Qur'an 569/23
kuhama kwake Makka 347, 348/40
adui zake walijengesha msikiti 360, 361/107
kuitwa mchawi 366/3
hakuacha sehemu ya Qur'an 401, 402/13
ni mfano kamili 738/22
wakeze ni miongoni mwa Ahlul-Bait 417/74
ghera yake juu ya Mungu 421/93
angeweza kuwa mwana wa Mungu 855/82

kuomba kwake msamaha 824, 825/56; 881, 882/3
hakutunga Qur'an 964, 965/4
mfano wa Musa 328/53; 568/10; 569/21; 589/49; uk. 901; 992/16
aliwasusia Sahaba watatu 363/118
Mungu anamsifu 365/128
kulinganishwa na Isa 1018/2
ni jua 748/47; 1045/2
kusingiziwa na wanafiki 743-745/38
si baba wa kimwili wa mwanamume ye yote 745-748/41
wakeze wanaitanguliza dini 749/52
wakeze wasiolewe tena 750/54
kuondoka kwake Makka na kurejea huko 700/86; 1049/2
wenye kumwudhi watalaaniwa 351/61; 751/58
maana ya kumsalia 751/57
matokeo ya uadui naye 759/32
ni mwanadamu mkamilifu 772/2; 916/4
Mungu hakumwacha 1049/4
alitunga shairi 779/70
hakutaka malipo kwa watu 256/91; 447/105; 624/73; 842/24
hakupotea 1050/8
maadui zake kutupwa motoni 176/116; 862/8
alifanana na Mitume wa kale 868/10
alirahisishiwa mzigo 1051/3, 4
wafuasi wake 99/32; 123/111; 162, 163/70; 165/81; 874/3; 883/11
alizuiwa kufanya Haji ndogo 885/19; 886, 887/28
adabu mbele yake 888/2
mashahidi wake wa maana 463/44
hakufundishwa na mtu 504, 505/104
safari yake ya njozi 520/61
hakwenda mbinguni na kiwiliwili 525/94
alikutana na Musa 545/66
ni mwanadamu tu 554/111; 886, 887/28
adui zake wanababaika 584/4-6
alibadili hali ya watu 655/64
kuchukua kwake baraka za Qur'an 1076/3
huruma yake kwa makafiri 657/4
alionya hata jamaa zake 672/215
adui zake wakubwa 681/49
hirizi kwa watu wa Makka 684/73
babaake mdogo hakusilimu 695, 696/57
hakujua kusoma wala kuandika 303/158; 308, 309/159; 708/49; 846/53
ulimwengu ulijaa ufisadi kabla ya ujaji wake 719/42
wakeze ni mama za waaminio 735/7
hakuoa kwa sababu ya anasa 740, 741/29
wakeze kupokea malipo makubwa 741/32
wakeze walitakaswa 742/34
akikata shauri lifuatwe tu 743/37
mtumishi wake hakutaka kumwacha 743, 744/38
hakusifu miungu 907, 908/20-22
alipasua mwezi 911/2
ndiye Roho wa kweli 938/23
si mwehu 972/3; 973/7
malipo yake hayakatiki 972/4
ana tabia njema tukufu 133/160; 365/128; 672/216; 887/30; 972/5; 1018/2
hali ya maadui wake 973/11, 17
dalili za ukweli wake 374, 375/17; 980/46; 990/27
watu walitaka kumwangamiza 989/20
aliona hofu 991/2, 6
ahadi zake zitatimia 1006/8
Mungu pamoja naye 1049/2
wakati ujao ni bora kwake 1049/4, 5
alikuwa yatima 1050/7
alipanuliwa kifua chake 1051/2
ametajwa katika 'mji wenye amani" 1052/4
atiiwe na waaminio 160, 161/60; 162/66; 947/13
ametajwa katika Qur'an 129/145; 745/41; 874/3; 887/30
aliteremshiwa Qur'an 11/24; 486/88; 494/45; 671/194, 195; 874/3
ametajwa katika Biblia 31/102; 303-308/158; 758, 759/31; 869/11
aliinuliwa kwenye cheo kilichosifika 523/80
ni Mtume wa Mungu 78/253; 772/4; 868/10
Manabii wa zamani walimwamini 17/82
aliwasikitikia watu hadi ya kujiangamiza 530/7; 657/4; 765/9; 1050/8

kazi zake kubwa nne 38/130; 951/3
hakujua ghaibu 248/51; 597/110; 752/64; 971/26, 27; 1017/43-45

Musa:
fimbo yake 294/108; 569/21
kaitwa mchawi 295/110; 390, 391/77
adhabu kwa maadui wake 297/131; 298/134
mbao zake 300/146
safari yake ya kiroho 542-550/61-83
alikutana na Mtume 545/66
aliona moto 568/11; 675/9
dua yake 393, 394/89
ishara zake tisa 526/102; 675/13
Firauni alimzulia 572/58
hofu yake 573, 574/68; 658/13
hakudhamiria kuua 659/21
alimwomba Mungu amsitiri 689/17
alimsusia Samiri 578/98
alikuwa mwaminifu 691/27
mwujiza wake wa kuvuka bahari 858/25
mama yake alipata ufunuo 570/40; 688/8

Mwanadamu:
anafuata wazee wake 48/171; 229, 230/105; 663/75
afuate uzuri, sio wingi 228/101
hali ya kuumbwa kwake 599/6
maendeleo yake ya kiroho na ya kimwili 616, 617/3-15
anayo asili ya Kiislamu 717, 718/31
amefanana na mbegu 258/96
achochewa na hofu na tumaini 371/8
kaacha njia ya mwongozo 375, 376/20
akifanya wema atapata nyongeza pia 157/41; 377, 378/27
akifanya ubaya atalipwa sawa na ubaya 378/28
namna mbili za wanadamu 1067/2
kupotezwa bila elimu 263/120
kuishi ardhini tu 279/26
haongoki kwa elimu peke yake 379/32
ajifaidishe na neema za Mungu 400/7
hawezi kuepukana na maovu 437/54
akishika njia ya ubaya hunyimwa rehema 453, 454/12
hakuachwa bila ufunuo 498/69
kwa vitendo anajivutia shari 512/12-14
Nabii pia ni mwanadamu 554/111; 618/25
asifuate mila, bali Mungu 704, 705/26
asiwe na marafiki wabaya 707/42
afanye juhudi inayofaa 712/70
udhaifu ndiyo hali yake 154/29; 721/55
amepewa hiyari ya kuchagua 730,731/14
aweza kuvumilia mashaka 753/73
ni mhitaji wa Mungu 766/16; 880/39
namna anavyoongoka 769/33
asafiri na kuona mwisho wa wabaya 828/83
wema wake haumnufaishi Mungu 835/47
aonywe juu ya Kiyama 839/8
shabaha ya kuumbwa kwake 862/13, 14; 900/57
ameumbiwa vitu vya duniani 867/4
amkimbilie Mungu 900/51
alipe wema kwa wema 920/61
afikriye ya kesho 942, 943/19
anadhani Mtume hataletwa 988/8
asili ya wanadamu wote ni moja 1007/21
asiwe mpunjaji 1026/2
ashike njia ngumu 1044/12

Mwenyezi Mungu:
sifa zake 3, 4/2-4; 728/35; 928, 929/4-7; 929/10; 943/24; 968/2-6
kupiga muhuri 8/8; 390/75
Majina Yake 14/32; 313/181; 528/111
maana ya 'Amri Yake' ni adhabu pia 488/2
hana mke 259/102; 987/4
hasinzii wala halali 80, 81/256
rangi yake 39, 40/139
hachoki 80/256; 893/16; 895/39
haamrishi maovu 279/29
kumkumbuka 44/153; 326/46
kundi lake litashinda 215/57; 938/22
hasahau 563/65; 572/53
hujaribu watu wake 44/156
hali chakula 240, 241/15
anatutakia mepesi 54/186
atafufua wafu 481/24; 725/17; 773, 774/13; 895/44
yu karibu nasi 55/187; 893/17
alama zake 199 - 200/3

alimlinda Mtume 218/68
maneno yake hayabadilishwi 244/35; 262/116; 388/65
Ishara zake zisifanyiwe mzaha 251/69
mioyo hutulia kwa kumkumbuka 459/29
fikara za watu si dini yake 464, 465/4
wenye kukataa mamlaka yake hawapati malipo 469, 470/19
huongoza watu 258/97
macho hayamdiriki 260/104
husema na wenye kustahili 264/125
huwaongoza wenye mioyo safi 264/126
ataleta ushindi wa Islam 345/33
huwapa watu muhula wa kutubu 372, 373/12
washiriki wake hawatajiki 461/34
siku zake 465/6; 863/15; 981/5
fadhili zake wagawiwe watu 473/33
anawasaidia watu wote 513, 514/21
ni Mwumbaji wa roho pia 524/86; 617/15
anao uwezo wa kuleta na kuzuia maji 617, 618/19
maneno yake huwafanya wabaya kuwa wema 765, 766/13
wenye elimu ndio humcha 707/44; 768/29
hana utatu 219-222/74
ngamia wake 288/74
awe mpenzi kuliko kila kitu 338/24
anamsifu Mtume 365/128
Kiti chake cha Enzi 367-369/4
anaita kwenye Nyumba ya Amani 377/26
wana wa Mungu 35/117; 206/19; 259/102; 340, 344/30; 558/24; 566/89-93; 587/27; 792/152, 153; 855/82
anaona vikubwa na vidogo 386, 387/62
rafiki zake hawana hofu 387, 388/63
huwaletea njozi na wahyi rafiki zake 388/65
anasema 576/90
ghairi yake asitiiwe 398/107; 455/15
ni hakimu bora 398/110
Enzi yake iko juu ya maji 400, 401/8
laana yake kwa wadhalimu 404, 405/19, 20
habadili mwendo wa rehema ila watu wanapobadilika 453, 454/12
hupokea maombi ya makafiri pia 455/15
daraja za kuumba kwake 467, 468/11
hatari za kukosa shukurani juu ya neema zake 506, 507/113, 114
faida za kumwogopa 919/47; 961/6
sifa zake huonekana wakati wote 923/30
anakuza mwili na roho pia 925/58
uumbaji wake hauna upungufu 968/5
humweka mtu kaburini 1019/22
atamfufua mtu 1019/23
yu mkali wa kuadhibu 1024/7
ni mjuzi wa ghaibu wa pekee 80, 81/256; 99/30; 386, 387/62; 568/8; 683/66, 67
amewaridhia sahaba za Mtume 359/100; 363/117; 1061/9
amenunua mali na nafsi za waminio 362/111
ni Mmoja tu 273/164; 455, 449/17; 495/52; 647/3; 1076/2
hana mfano wake 499/75; 840/12; 1076/5
ameyafanya maji kuwa chanzo cha uhai 587/31
cha Mungu ni bora 619/28; 696/61
alileta Mitume baada ya Taurati 621/45
huinua dhaifu 688/6
ahadi yake 696, 697/62
amelinda Makka 711/68
uwezo wake katika hitilafu za rangi na lugha 716, 717/23
imani kwa sifa zake hukomesha maovu 734/2
ni Mwenye shukurani 769/35
viapo vyake 772/3; 781/2-4
hana binti 792, 793/150 - 161
Roho yake ni 'Wahyi' 803/73; 819/16
aliangamiza waasi wa zamani 796/12-15; 820/22
husaidia Manabii wa waaminio 824/52
kumwomba huzidisha imani 825/61
haadhibu watu Nabii akiwa kati yao 835/46
anajua wakati wa Kiyama 836/48
njia tatu za kusema na waja wake 846/52
atayahukumu mataifa 864, 865/29; 1032/14
utukufu wake utaonekana siku ya Kiyama pia 866/37
maneno yake ni msingi wa imani 867/5
ataharibu kazi ya wapingaji haki 874/2

aleta mapenzi 945/8
kuonyesha njia mbili 1043/11
alikuwa pamoja na Mtume 1049/2
atawaadhibu wasingiziaji, wasengenyaji na wakusanyaji wa mali 1068/2-5

Nabii:
dalili za ukweli wake 162, 163/70; 374, 375/17; 404, 405/19; 573/62; 980/46; 990/27
mwenye kukataa Nabii mmoja anawakataa wote 183/151
na Mtume ni kitu kimoja 562/52
asiyeleta sheria mpya 212/45
misiba hufuata ufikaji wake 292/95; 513/16
anatakiwa wakati wa uovu kutapakaa 1060/3
hatangulii kushambulia maadui 295/117
haachi kazi yake kwa kupewa rushwa 385/56
anakataliwa kwa sababu mbili 390/76
hatumii uongo na udanganyifu 391/83
adui zake hupata hasara 405/23
wa kweli anabainisha 406/26
apimwe kwa mizani ya kweli 406/28
huwa na ghera juu ya Mungu 421/93
hatendi dhambi 418/79; 432/25; 442/78
aweza kufanya kazi chini ya serikali isiyoshika dini yake 438/56; 442/77
asiwaombee washirikina 362, 363/113, 114
huchekwa na maadui 542/57; 775/31
huondoa desturi na tabia mbaya 573/64
anakula chakula 585/9; 643/8
kuitwa mwana wa Mungu 587/27
ni mwanadamu 554/111; 618/25; 886, 887/28
dua baada ya kupona katika balaa ni tabia yake 619/30
maombi ndiyo silaha yake 620/40
wito wake sio wa watu wengine 646/64
wadhifa wake ni nzito sana 658/13
lazima ashinde 793/172; 811/40; 817/5
kumkadhibisha mkweli ni dhuluma kubwa 810/33
kila mmoja hakutajwa 827, 828/79
shauri la kupewa unabii haliwahusu watu 850/33
anafanana na wenzake 868/10
watu wanamkataa 984/8
hutumia njia zote za kuwaokoa watu 985/9, 10
dua yake mbaya haipotei bure 986/27
atiiwe 162/65, 66
mwanamume tu anakuwa Nabii 448/110
hakati tamaa 448, 449/111
ana subira 468/13
wa uwongo sheria yake inapotea 472/27
kuomba kwake msamaha 475/42
kazi yake ni kufikisha 226/93

Nafsi:
ina tamaa 178/129
namna zake tatu 998/3
kuitakasa 1045/10

Naml:
maana yake 676/19

Neema:
za kiroho 5/7
za peponi 12 /26; 424-425/109; 461, 462/36; 876, 877/16; 1003, 1004/18, 19; 1032/12
za kiroho na za kidunia 207/21
mtu ajifaidishe kwazo 400/7
hasara za kukosa shukurani juu yake 506/113
watu wakighairi, hunyimwa 328/54
za peponi ni bora 731/18
za Mungu hazileti athari mbaya 903/30

Ngamia:
wa Nabii Swaleh 288/74; 415/ 65, 66; 668/ 156-159
alikatwa miguu 289/78; 415 , 416/66-69; 668/ 158, 159; 913/28-32
kuliwa nyama yake 268/145
kuingia katika tundu la sindano 282/41

Ng'ombe:
amri ya kumchinja 24/68
ndama wa Samiri 576/89; 578/98
halali kuliwa nyama yake 268/145

Nguo:
mke na mume ni kama nguo 55, 56/188

makusudio yake 279/27

Nguruwe:
uharamu wake 48-50/174; 200/4; 269/146; 507/116
baadhi ya Mayahudi kugeuzwa kuwa nguruwe 215, 216/61

Nuhu:
Mungu alimchagua 100/34
alitumwa kwa watu wake 285/60; 406/26; 618/24; 703/15; 984/2
habari zake 285, 286/60-63; 406-411/26-49; 618, 619, 608/24-30; 665, 666/106-121; 786/76-83; 912/10-17; 984-986/2-29
ndani ya habari zake mna bishara 412/50; 619/31
Ibrahimu ni katika wafuasi wake 786/84
utume wa Kitabu katika kizazi chake 933/27
kumkataa ni kuwakataa Manabii wote 665/106
safina yake imebaki kama ishara 912/16
ametajwa katika "Zeituni" 1052/2

Nusuk:
maana yake 273/163

Nyani:
baadhi ya Mayahudi kugeuzwa kuwa manyani 23/66; 215, 216/61

Nyota:
kukosa nuru 1006/9
kuanguka 906/2

Pepo:
neema zake 12/26; 353/72; 461, 462/36; 536/32; 769/34-36; 783, 784/42, 50; 854/71-74; 860/53-58; 876, 877/16; 902, 903/18-25; 919- 921/49-78; 923, 924/16-39; 1003, 1004/13-22; 1008, 1009/42-44; 1027/23-29; 1032/12
ya ardhini 15/36
neema zake ni za milele 424-425/109; 461, 462/36; 553, 554/108, 109; 563/62; 648/16; 894/35
neema zake ni tofauti na za hapa duniani 731/18; 876, 877/16
ni mahali pa amani 483/46, 47; 563/63; 778/59; 860/52
kuozwa wake peponi 96/16; 902/21
sifa za watu wa peponi 150/14; 563/61; 894/32-34; 903/27-29; 982, 983; 23-36; 1016, 1017/41, 42
waaminio watapata humo kila watakacho 649/17; 778/58; 833/32; 854/72; 895/36
wamchao Mungu watapata pepo mbili 919/47; 920/63
waaminio hawatatolewa humo 483/49
neema zake zimeelezwa kwa mfano tu 461, 462/36; 876, 877/16
ina wasaa sana 932/22
hamna taabu yo yote 483/49; 769/36
hamna joto wala baridi kali 1003/14
hamna upuuzi 563/63; 903/24
hamna kifo tena 860/57
hamna kuleweshwa 784/48; 923/20
hamna umbali na Mungu 554/111; 777/56; 1001/23, 24
malaika watawaamkia wakazi wake 458/24, 25
amri ya kuitafuta 128/134
ni ahadi ya Mungu kuileta 461, 462/36; 563/62; 649/17; 833/31; 875/7; 876, 877/16; 894/33

Pombe:
tazama "Ulevi"

Punda:
sauti yake inachukiza 726/20
kubeba vitabu 952/6

Qiblah:
maana yake 393/88

Qur'an:
herufi zake zenye kutamkwa mbalimbali 6, 7/2,3; 274/2; 366/2; 428/2; 450/2; 555/2; 567/2; 657/2; 674/2; 687/2; 772/2; 795/2; 817/2; 838/2,3; 888/2
haikutengenezwa na Mtume 9, 10/17
haina mfano 11/24; 402/14, 15; 904/35
inasadikisha vipi Biblia 16/42; 732/24; 869/13
kuuza aya zake 26/80
aya zake hazitanguani 32-34/107; 330, 331/67; 504/102; 809/24
uzuri wake 34/114; 359/99; 767/25
ni nzuri kuliko Injili 52/180; 226/91

inaipita Biblia 80, 81/256; 895/39
haileti karaha katika dini 81/257
ina sheria nzuri juu ya deni 89, 90/283
inaihifadhi Biblia 213/49
haileti matusi 215, 216/61
masimulizi yake ni utabiri 242/26; 412/50; 579/100
mpango wake una hekima 255-256/85-87
ni nasaha na ponyo 385, 386/58; 835/45
imetaja habari isiyojulikana zamani 394, 395/93
ndiyo **Elimu** 395/94
inaeleza daraja za uumbaji 467, 468/11
imechukua maelezo ya maendeleo ya mtu 616, 617/3-15
imeeleza hitilafu nyingi za wana wa Israeli 684/77
haikatai miujiza 244, 245/36; 709/51, 52
sifa zake 284/53; 459, 460/32;
Kiarabu kuwa lugha yake 371/8
hoja za ukweli wake 380-381/38, 39
upinzani wa padre Dale umejibiwa 9, 10/17; 16, 17/43; 34-34/107; 35/116; 78, 79/254; 80, 81/256; 87, 88/276; 89, 90/283; 112, 113/62; 139-142/196; 144-147/4; 233-236/117; 240, 241/15; 244, 245/36; 254-256/85-87; 319, 320/13; 430, 431/18; 443, 444/81; 497/68; 519, 520/60; 596/107; 713 - 715/5; 987/2; 1050/8
kulindwa kwake 399/2; 401, 402/13; 477, 478/2; 478, 479/10
kulinganishwa na Biblia 478, 479/10
ni mkono mweupe wa Mtume 569/23
kuachwa kwake 650, 651/31
ni nuru 464/2; 808, 809/23
ni kama mti mzuri 471/25, 26
jina lake limetolewa na Mungu 477, 478/2; 486/88
inaeleza madaraja ya wema na uovu 501, 502/91
itaeneza elimu 587/31; 776/37; 900/50; 1057/2-6
haikutaja siri ya Mtume 964, 965/4
kukusanywa kwake 999, 1000/17-20
hakuna sheria baada yake 449/112
ni Adh-dhikr 494/45; 850/37
ni Furqaan 647/2
ilipangwa na Mtume kwa amri ya Mungu 651/33
iliteremka katika usiku wa Heshima 856/4; 1059/2
ina mambo yote mazuri 1060/4
faida ya sura zake za mwisho 964, 965/4
haikutungwa na Mtume 964, 965/4
haikufundishwa na mtu 504, 505/104
mfuasi wake wa kweli atashinda 567/3
jihadi ifanywe kwayo 653/53
isifuatwe kwa upofu 656/74
haikuletwa na shetani 673/224
isomwe na kufuatwa 686/93
inapambanua 687/3
bishara zake zilizotimia 697 - 699/5
inaongoza maumbile ya asili 717, 718/31
inakomesha desturi mbaya za Waarabu 734, 735/5; 883, 884/12-14; 934/2
ni bora kabisa 813/56
ilipigiwa makelele 832/27
haikuteremshwa kwa mkuu wa kidunia 850/32
imeleta ujuzi juu ya kiyama 853/62
Hadithi zipatane nayo 861/7

Qureish:
maana yake 1070/2

Riba:
ubaya wake 87, 88/276
mayahudi pia walikatazwa kuichukua 193/162

Ruuhul Qudus:
maana yake 28/88; 195/172; 488/3

Saaibah:
maana yake 229/104

Sabaa:
maana yake 756/16

Sabato:
Mayahudi hawakuiheshimu 184/155; 310/164
adhabu ya kuivunja 23/66; 158, 159/48; 310/167; 508/125

Sadaka:
namna zake 7/4; 63/216
amri ya kuitoa 58/196; 956/11

hutolewa kwa siri na dhahiri 86/272; 87/275
juu ya kupenda mali 50, 51/178
ya wamchao Mungu hupokelewa 208/28
itolewe kwa kila hali 128/135
atoaye sadaka atapata raha 1047/6-8
Ismail alitolewa sadaka 789/113
Pia tazama "Mali"

Safaa na Marwa:
maelezo yake 45/159

Sala:
amri ya kuisali 615/78; 644/57; 993/21
maana ya kuisimamisha 7/4
vijana pia wahimizwe kusali 725/18
ya Tahajjudi 523/80; 991/3-7
ya Ijumaa 952, 953/10
nyakati zake tano 173/104; 522, 523/79; 715/18, 19
hali isiyokuwa ya sala 157, 158/44
kuiharakisha wakati wa hatari 173/102
ya jamaa katika hatari 173/103
isaliwe msikitini 280/32
ni alama ya Waislamu 457, 458/23
Nabii Isa alisali 559/32
kumsalia Mtume 751/57
watu wasizuiwe kwenda msikitini 34/115
faida yake 707/46
adhabu ya wenye kuipuuza 562/60; 997/43, 44; 1071/5, 6
usafi wa mwili kwa ajili yake 202/7
usafi wa mwili na fikara 157, 158/44
amri ya kuzichungua sala 74/239; 616, 617/10
unyenyekevu ndani yake 616/3
watu wa nyumbani waamrishwe kusali 562/56; 582/133

Saleh:
habari zake 288, 289/74-80; 414, 415/63-66; 485/81; 667, 668/142-159; 680/46; 913/24-32; 1046/12-15
alitumwa kwa watu wake 288/74; 680/46;
watu wake wameitwa "wenyeji wa Hijri" 485/81
alipewa ishara ya ngamia. (Soma habari zake chini ya "Ngamia").
adui zake tisa walitaka kumwua 681/49, 50
wapinzani wake waliangamizwa kwa tetemeko la ardhi 289/79; 416/68, 69; 668/159; 1046/15
wenye kumkataa walikadhibisha Mitume wote 913/24

Shaitani:
habari zake 157/39; 176, 177/118-122; 277, 278/21-23; 279/28; 519/54; 936/11
mtu mwovu ameitwa shetani 277, 278/21
maneno yake hupotea 611, 612/53
adui pia ni shetani 327/49
atakataa kusaidia wafuasi wake 470, 471/23
sifa za kishetani 598/4
hakusogea karibu na Mtume 673/224
waganga na makuhani ni mashetani 781/8
maana nyingine 785/66; 800/42
pombe na kamari ni kazi zake 226/91, 92
ni rafiki wa makafiri 279/28; 565/84
hana nguvu juu ya waaminio halisi 504/100, 101
tumwombe Mungu atulinde na shari yake 503/99; 626/98, 99; 1078/5

Shajarah:
maana yake 15/36

Shu'aibu:
alitumwa kwa watu wake 290/86; 419, 420/85
wenye kumkataa waliwakadhibisha Mitume wote 670/177
maadui zake waliangamizwa kwa tetemeko 291/92; 422/95
habari zake 290, 291/86-94; 419, 422/85-96; 670, 671/177-190

Shukurani:
maana zake 466/8

Siku ya Kiyama:
ahadi ya kufufua 12/29; 617/17; 919/48
ni rahisi kuileta 499/78
hata zamani watu waliikataa 243/30
wapinzani wake watapata hasara 406/23
ni tofauti na dunia hii 476/49

wasiotambua ishara hapa watakuwa vipofu akhera 522/73
mkazo juu ya kuiamini 526/99
maungo ya mtu yatasema siku hiyo 778/66
wakati wake anaujua Mungu 728/35; 836/48
watu waonywe juu yake 839/8
siku hiyo pia utaonekana ukubwa wa Mungu 866/37
vilivyoumbwa vitakoma siku hiyo 867/4
maisha ya kidunia siku hiyo yataonekana mafupi 873/36
ni siku ya hasara kwa makafiri na wanafiki 958/10
maisha ya baadaye ni bora kwa wamchao Mungu 164/78; 448/110; 514/22
maisha ya Akhera ndio maisha hasa 711/65; 823/40
haja yake 370/5
alama zake 1021, 1022/2-14

Suleiman:
alirithi elimu ya babaake 676/17
alipewa elimu na hekima na Mungu 593/80; 676/16
alipewa vyote alivyohitaji 676/17
maelezo mabaya ya waasi juu yake 31, 32/103
alitiishiwa upepo 593/82; 755, 756/13; 800/37
wapigaji mbizi walimtolea malulu (Bahrein na Maskati) 593/83; 800/38
mafundi wageni aliowaajiri
walimtengenezea majengo na madegi 756/14; 800/38, 39
watu wa milimani walitii amri yake 679/40; 800/39
namna tatu za majeshi yake 676/18
barua yake ya kumbashiria malkia 677/29-32
alitengenezesha kiti cha enzi kizuri zaidi kwa ajili ya malkia 678, 679/39-42
namna yake ya kubashiri 680/44, 45
sababu ya yeye kupenda farasi 799/32-34
alionyeshwa ndotoni hali mbaya ya mwanawe 756/15; 800/35
ombi lake la kuongezewa neema ya kiroho 800/36
alikuwa mnyenyekevu 799/31
cheo chake 800/41

Talaka:
sheria kuhusu talaka 69, 70/228; 748/50; 931, 932/2
maelezo zaidi juu yake 69-74/228-243; 960-961/2-8

Toba:
maana yake 151/18, 19; 399, 400/4; 421/91; 507/120

Tuur:
kunyanyuliwa kwake 23/64

Uadilifu:
baina ya wake 178, 179/130
amri juu yake 180/136; 203/9; 271/153; 501, 502/91; 798/27; 889/10
Mitume na Vitabu huletwa kwa kuusimamisha 932/26

Ubadhirifu:
amri ya kuuacha 515/27, 28, 30

Ubahili:
pengine ni kwa sababu ya kiburi 156, 157/37-39; 932/25
ni kujinyima 854/39
Sahaba hawakuwa nao 941/10
kuuacha ni kufaulu 941/10; 959/17
ni kujiitia tabu 513/30; 1047/9-11

Ugomvi:
njia ya kuuamua 889/10, 11
wanafiki hawapeleki kesi zao katika mahakama za kidini 161/61; 642/48, 49
waaminio watii hukumu zilizotolewa na wakubwa wao 162/66; 643/52; 743/37

Ukhalifa:
umeahidiwa kwa wenye kuamini na kutenda matendo mazuri 643, 644/56
Mungu aliutoa zamani 13/31; 798/27
Haruna kuwa Khalifa wa Musa kwa muda 299/143
sifa za maimamu 732/25
wavunjao amri ndio wataukana 643, 644/56; 731/19 (maana ya fasiki)

Ulevi:
hasara zake 65-67/220; 157, 158/44

U.N.O.
kufuata agizo la Qur'an 57/194

Uombezi:
kwa idhini ya Mungu 80, 81/256

Upole:
umehimizwa 571/45

Urithi:
wasioweza kuupata 52/181
mafungu ya warithi
kwa ndugu wa damu tu 332/76

Utume:
kupatikana katika umati huu 5/7; 931/20
wadhalimu hawaupati 36/125
usiokuwa wa sheria 281, 182/36

Utumwa:
ukomeshwe 636-639/34; 875/5
watumwa wapewe uhuru 170, 171/93; 934/4; 1044/14

Uzeir:
habari zake 340/30

Uzinifu:
msiukaribie 516/33
adhabu yake 629, 630/3

Viapo:
vya upuuzi 69/226; 781/2-4
vya Mungu 502/92; 772/3; 911/2
visitumiwe vibaya 502, 503/93, 95

Viatu:
katika ndoto ni ahli 568/13

Vita:
ya kujilinda 56/191; 335/6
kwa kukomesha mateso ya kidini 57/194
ilichukiwa 64/217
waaminio wasimame imara vitani 329/58-61
adui akitoa amani vita iachwe 330/62
mateka wasichukuliwe bila vita 331/68
waliovunja ahadi wapigwe vita 334, 335/5
wakati wa vita hakuna urafiki na makafiri 182/145; 944/2
kwa kusimamisha uhuru wa dhamiri 324/40
kugawanya mali iliyopatikana vitani 325/42
habari za vita ya Badri 325, 326/44, 45; 650/26; 709, 710/56; 762/52; 914, 915/46
habari za vita ya Hunain 338, 339/25
habari za vita ya Handaki 736/10; 796/12
silaha zilikosekana 357/92
ya tatu ya ulimwengu 541/54

Wafu:
wanaishije 44/155
hawarudi duniani tena 595/96; 627/101; 775/32; 812/43
kusemeshwa 459, 460/32
wa kiroho 245/37; 258/96; 321/25
nyumba za makafiri kuitwa makaburi 983/44

Waislamu:
sifa za waaminio 128/135, 136; 616, 617/2-12; 640/37, 38; 655, 656/64-78; 742, 743/ 36, 37
maamkizi yao 169/87; 645/62
waseme vizuri 27/84
wakiacha dini yao hawauawi 64/218; 118/87-90; 180/138; 214, 215/55; 506/107-111
wapatanishe watu 175, 176/115; 889, 890/11
washindane katika mema 43/149; 1014/2-6
wasigawane 271/154; 687/5; 840/14
matokeo ya kuwacheka 627/111
wapinzani hawafaulu 628/118
wamwombe Mungu msamaha 628/119
wanaweza kutunga shairi zuri 673/228
wasijadiliane na wabishanaji 708/47
hawaruhusiwi kueneza ubaya 183/149
washike desturi hii ya kuhubiri 252/72
wajiepushe na kila uovu 263/121
maadui wao hawatafanikiwa 266/136
waamrishe mema na kukataza maovu 123/111; 223/80
wameahidiwa Ukhalifa 643, 644/56
nasaha kwao 327/48, 49

wajiweke tayari kwa vita 329/61
wakubali amani 330/62
wasaidiane 332/74
wanaweza kupata utukufu tena 373, 374/15
wamtegemee kwa ushindi 427/124
kusema "Mungu akipenda" 446/100
alama zao 457, 458/21-25
watajaribiwa 44/156; 463/6; 564/72, 73; 701/3
wa kweli watapata ushindi 128/140; 468, 469/15; 567/3; 615/79; 879, 880/36
na Wakristo watavyolingana 536-539/33-45
wazuie uovu kwa wema 626/97
waombe idhini wakitoka mkutanoni 645, 646/63
wawe na ghera 215/58, 59
wahame 710/57
waliahidiwa nchi nyingine 740/28
washike fundisho lifaalo wakati 808/19; 1032/12
wanashukiwa na malaika 833/31, 32; 869/14
waite wengine kwenye dini 833/34
hushauriana 844/39
wasiwe walegevu 128/140; 879, 880/36
washike imani na utawa 880/37
wapeleleze habari walizoletewa 889/7
wameahidiwa utume 931/20
wasijitenge na dunia 933/28
washike adabu za mikutano 936, 937/12
wasifanye urafiki na makafiri katika vita 182/145; 944/2
watende sawa na kauli zao 948/3
watoe mali na watoto katika njia ya Mungu 956/10
wajihadhari na wake na watoto 959/15
wamefananishwa na mabibi wawili 967/12-13
wasafiri katika ardhi 969, 970/16
mambo yenye kuwafanikisha 1014/2-6
wanalindwa na malaika 1034/5

Wakristo:
hila za mapadre iv, v, vi
wamegeuza Injili 17, 18/43; 204/14
wa Najran 34/115
wataendelea na imani juu ya kifo cha laana 192, 193/160;
watachukiana wao kwa wao 204, 205/15
wataadhibiwa wasipotubu 206/19
wamfuate Mtume 213/48; 217, 218/67
imani yao ya kisasa ni upagani 223/78; 340-344/30;
wema kati yao 224/84
wanangoja adhabu kali zaidi 232, 233/115, 116
baadhi ya makosa yao 233-236/117
wanawaheshimu wakubwa wao kama Mungu 344, 345/31
mapadre wengine wanachukua mali bila sheria 345, 346/34
wanatamani wangekuwa na mafundisho kama ya Uislamu 478/3
kupenda sana mbwa 533/19
wa kweli kusumbuliwa 535/26
kutanabahishwa 555/5
hawakuamrishwa uruhubani 933/28
wamepewa sehemu ya Kitabu 158/45
washirikiane na Waislamu juu ya umoja wa Mungu 114/65
hali zao 115/73; 116/79
uzuri wao 116/76; 224, 225/83, 86
Utatu hautawaponesha 1008/31, 32
wanategemea kifo cha Yesu 1024/7

Wanafiki:
ni waongo 954/2
kiongozi wao 955/9
wanakutana kwa siri 935, 936/8, 9
alama zao 181, 182/143, 144; 355/79
adhabu yao 182/146
hawatekelezi sala wala hawatoi zaka 350/54
wasitendewe kwa ulainifu 354/73
wasisaliwe 356/84
walimzulia Bi Aisha 631, 632/12

Wanawake:
ni kama nguo 55, 56/188
washirikina wasiolewe 67/222
wasiingiliwe katika hedhi 68/223
ni shamba lenu 68, 69/224
kutengana nao 69/227

wasitaabishwe kwa sababu ya watoto 72/234
wameheshimiwa katika Uislamu 139, 140/196; 496/60
katika Ukristo 139 - 143/196
kuwaoa zaidi ya mmoja 144-147/4
wana malipo sawa na wanaume 177/125; 742, 743/36
wasisumbuliwe 178, 179/130
Uadilifu baina yao 178, 179/130
mama wa kambo ni mama pia 446/100
kujisitiri 516/33; 634, 635/31, 32; 751, 752/60
wenye kuwasingizia 630/5
wenye kusingizia wake zao 630/7-10
wamtii Mtume 947/13
wasiwe laini katka mazungumzo 741/33
kupewa binti ni fadhili ya Mungu 845/50
washirikina hawakupenda mabinti 848/18
wa peponi 902/21
wasiachwe wakiwa katika hedhi 960, 961/2
huzaa kwa amri ya Mungu 845, 846/50, 51
mfano wa mwanamke mjinga 502, 503/93
mfano wa mabibi waaminifu 967/12, 13
kisa cha mke wa waziri 431-434/22-35
wanawake wazee hawakulazimika kujifunika 644, 645/61
malkia wa Sheba 677-680/24-45
mama wa Musa alifunuliwa na Mungu 570, 571/40, 41; 688, 689/8-14
mkewe Musa 690, 691/24-30
wakeze Mtume s.a.w. 417/74; 735/7; 741/32; 742/34; 749/52; 750/54

Wasabii:
ni nani 22/63

Wasiila:
maana yake 210/36
mnyama 229/104

Wathamudi:
habari zao 288/74

Watumwa:
katka Biblia 139-143/196
wapewe uhuru 636-639/34

Wayahudi:
uzuri wa baadhi yao 116/76
hila zao 115/73; 116/79
walipewa sehemu ya Kitabu 158/45
walivunja mapatano 739, 740/27; 939/3
Myahudi kaamini 701/3
kuharimishiwa mafuta 269/147
washirikiane na Waislamu juu ya umoja wa Mungu 114/65
wanapenda sana uwongo 211/42; 211/43
hawakugeuzwa sura 23/66; 215, 216/61
walimsingizia Mariamu 184/157
wameahidiwa adhabu Akhera 206/19
Manabii wengi waliinuliwa kati yao 212/45
wamfuate Mtume 217, 218/67
walilaaniwa na Daudi na Isa 223/79
wawaulize Waislamu juu ya Qur'an 395/95
waliadhibiwa mara mbili 511/6-8
watavunja mapatano yao na Mtume 547/77
kutanabahishwa 555/5
hawadumu katika Falastini 596/107

Yahya:
habari zake 101/40; 556, 557/8-16

Yaajuja na Maajuja:
ni mataifa ya Kikristo 554/111
watashika palipo pazuri 595/97

Yakini:
faida yake 450, 451/3
daraja zake 1066/6
dhana haifai kitu 380/37

Yakubu:
nabii Ibrahimu alijulishwa juu yake 411/72
alijinyima baadhi ya vyakula 119/94
hakupofuka macho 444/85

Yatima:
wasaidiwe mali 63/216
ni ndugu zenu 67/221
mali yao iangaliwe vizuri 144/3; 148/7; 149/11; 271/153; 516/35
makafiri hawakuwaheshimu 1041/18
Mtume alikuwa yatima 1050/7
wasikemewe 1050/10
kuoa zaidi ili kuangalia mayatima 144, 147/4; 178/128
alishwe 1003/9

Yunus:
alikuwa mtume 194/164; 254, 256/87; 791/140
pia anaitwa Dhun-nuun (Mwenye samaki) 594/88
pia anaitwa Swaahibul-Huut (Mwenzi wa samaki) 976/49
anafanana na Nabii Isa na Mtume Muhammad 396/99
habari zake 791, 792/140-149; 976/49-51

Yusuf:
habari zake 428-447/5-101
alidhaniwa kuwa Nabii wa mwisho 822/35

Zaburi:
bishara zake 596/106
Daudi alipewa Zaburi 519/56

Zaka:
maelezo yake 351/60; 829, 830/7, 8
kwa waliozuiwa katika njia ya Mungu 87/274
amri ya kuchukua 360/103

Zakariyya:
habari zake 101/38-42; 555-557/3-12; 594/90, 91



1. SURA AL-FAATIHA

Muhadithina wengi wanaeleza ya kuwa sura hii nzima ilishuka Makka, na toka mwanzo ilikuwa ni sehemu ya maombi ya Waislamu. Hii ndiyo sura iliyotajwa katika aya ya Qur'an, *Na kwa yakini Tumekwisha kupa (Aya) saba zisomwazo mara kwa mara na Qur'an kubwa* (sura 15:88), ambayo ilishuka Makka. Habari zingine zinaeleza ya kuwa sura hii iliteremshwa tena mara ya pili, Madina. Sura hii ilishuka mapema tu Mtume s.a.w. alipoanza kazi.

MAJINA YA SURA HII NA MAANA ZAKE.

Jina maarufu la sura hii ni Faatihat-ul-Kitaab (Inayofungua Kitabu) (Tirmidhi na Muslim). Baadaye jina hilo lilifupishwa kuwa *Surat-ul-Faatihah*, au *Al-Faatiha.*
Sura hii imepewa majina mengi, na haya kumi ndiyo yaliyo sahihi zaidi: *Al-Faatiha, As-Salaat* (Sala), *Al-Hamdu* (Sifa zote njema), *Ummul-Qur'aan* (Mama ya Qur'an), *Al-Qur'aan-ul-Adhiim* (Qur'an Kubwa) *As-Sab'ul-Mathaani* (Aya saba zinazosomwa mara kwa mara), *Ummul-Kitaab* (Mama ya Kitabu), *Ash-Shifaa* (Ponyo), *Ar-Ruqya* (Kago), *Al-Kanz* (Hazina).

AL-FAATIHA IMETAJWA KATIKA AGANO JIPYA.

Inapendeza kuona ya kwamba jina *Faatiha* linapatikana katika Agano Jipya. Katika kitabu cha Ufunuo 10:12 mmeandikwa: "Kisha nikaona Malaika mwingine mwenye nguvu akishuka kutoka mbinguni ..... na katika mkono wake alikuwa na kitabu kidogo kimefunguliwa. Akaweka mguu wake wa kuume juu ya bahari, nao wa kushoto juu ya nchi." Neno la Kihibrania kwa *kufungua* ni *fatoah* ambalo ni lile lile la Kiarabu *faatiha*. Ufunuo 10:3-4 mmeandikwa: "Naye (Malaika) akalia kwa sauti kuu ....na alipolia zile ngurumo saba zikatoa sauti zake." Hizo ngurumo saba ni hizi Aya saba za sura hii ya *Al-Hamdu.*

YALIYOMO KATIKA AL-HAMDU.

Sura hii ndio utangulizi wa Qur'an. Nayo ni Muhtasari wa Kitabu chote. Hivyo, mwanzoni tu msomaji anajulishwa ni habari gani anazotazamia kuzipata katika Qur'an. Mtume Mtukufu s.a.w. alisema ya kuwa, sura ya *Al-Hamdu* ndiyo kubwa kuliko sura zote za Qur'an. (Bukhari).

Sura hii inacho kiini cha mafundisho yote ya Qur'an. Inaeleza kwa kifupi habari zote zilizoelezwa kwa urefu katika Qur'an. Sura hii imeanza kwa kuzieleza sifa zilizo msingi wa sifa zote zingine za Allah: zilizo msingi wa kuendesha ulimwengu na wa uhusiano baina ya Allah na mwanadamu. *Rabb* (Mwumbaji, Mhifadhi na Mlezi), *Rahmaan* (Mwingi wa Rehema). *Rahiim* (Mwingi wa Ukarimu). *Maaliki yaumi-d-Din* (Mmiliki wa siku ya malipo) - Sifa hizi zinaonyesha ya kuwa Allah alipokwisha mwumba.

mwanadamu akampa vipawa na uwezo ulio bora, na akamwekea njia, na vitu anavyohitaji kwa ajili ya kukuza mwili wake, makao yake, mwenendo wake na roho yake. Zaidi ya hayo akaweka kanuni ya kwamba kazi afanyazo mtu na juhudi zake zipate malipo ya kutosha.

Sura hii inaendelea kusema ya kuwa mtu ameumbwa kwa ajili ya 'ibadaat, yaani kumwabudu Allah na kupata kuwa karibu naye, na ya kwamba mtu daima anahitaji msaada Wake ili kutimiza hili kusudio kubwa la kuumbwa kwake.

Kisha sura hii inayo maombi yaliyokamilika yanayotosheleza kabisa haja zote za mwanadamu. Maombi hayo yanatufunza kuwa kila siku tutafute msaada wa Allah ili atupe kila kinachohitajiwa kwa ajili ya kutufanikisha katika maisha haya na ya baadaye. Na kwa kuwa mtu anaelekea kupata nguvu na kutiwa moyo kwa mfano mzuri wa watu wakubwa wenye heshima waliopitisha maisha ya kufanikiwa hapo zamani, ikabidi afundishwe kuomba ya kuwa kama vile watu wema wamchao Allah walivyofanikiwa kufikia makusudio ya maisha yao na kusaidiwa na Allah, basi naye pia Allah amfungulie njia za maendeleo ya mwenendo wake na roho yake.

Mwishoni, maombi hayo yanatoa maonyo ya kwamba hutokea mtu akapotea baada ya kuwa ameongozwa, naye akawa mbali na Allah. Tunafundishwa siku zote tujichunge na tumwombe Allah atulinde ili tusiteleze.

Hii ndiyo habari inayoelezwa kwa kifupi katika Al-Faatiha, na hii ndiyo habari inayoelezwa na Qur'an kwa wingi na kwa kutosheleza ikitoa mifano kadha wa kadha ili kumwongoza msomaji.

Seyyidna Ahmad (amani juu yake) amesema, "Sura Al-Faatiha ni mwujiza. Ndani yake mna maamrisho na makatazo, na bishara pia. Qur'an Tukufu ni bahari kubwa. Jambo lo lote linalotakiwa kutolewa humo, basi inatakiwa kuifikiria sana sura Al-Faatiha; maana sura hii ni *Ummul-Kitaab* (Mama ya Kitabu), na tumboni mwake hutoka mambo mengi" (Al-Hakam). Tena Mwanzilishi huyo Mtakatifu wa Jumuiya ya Waislamu wa Ahmadiyya akasema; "Kuisoma sura ya Al-Faatiha na Qur'an kwa mwelekeo na nia safi, kunasafisha moyo, na kuondoa mapazia ya giza, na kunafungua kifua; na kwa kumvutia mtafuta haki kwa Allah, anapatiwa nuru na baraka zinazowahusu walio karibu na Allah, ambazo mtu hawezi kuzipata kwa njia nyingine" (Barahini Ahmadiyya, jalada 1).

DUA KABLA YA KUSOMA QUR'AN

Waislamu wamelazimishwa katika Qur'an (Sura 16:99) ya kuwa wakati wa kusoma Qur'an wasome dua ya kujikinga na Shetani. Na Mtume s.a.w. alifundisha dua hii; *A'uudhu billaahi minash-shaitwaanir-rajiim* yaani, Najikinga kwa Mwenyezi Mungu anilinde na Shetani anayepigwa mawe. Kujikinga huku kunatarajia mambo matatu: (1) Ubaya usitufike; yaani tusikosee fundisho lo lote la Qur'an kwa sababu ya udhaifu au kupuuza au kwa sababu ya matokeo ya dhambi zetu, au kwa sababu ya kuwa na watu wabaya. (2) Wema usituponyoke; yaani tusishindwe kufahamu sawa sawa fundisho lo lote la Qur'an. (3) Baada ya kupata wema tusiangukie katika uovu; yaani baada ya kufahamu mafundisho ya Qur'an tusiangukie tena katika ujinga.

سُوْرَةُ الْفَاتِحَةِ مَكِّيَّةٌ وَّ هِيَ مَعَ الْبَسْمَلَةِ سَبْعُ اٰيَاتٍ وَّ رُكُوْعٌ

1. SURA AL-FAATIHA

Imeteremshwa Makka

Ina Aya 7 pamoja na Bismillahi

بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ ①

اَلْحَمْدُ لِلّٰهِ رَبِّ الْعٰلَمِيْنَ ② لَا

1. Kwa jina la Allah, Mwingi wa rehema, Mwingi wa ukarimu.

2. Sifa zote njema zinamhusu tu Allah Aliye Mola wa walimwengu wote.

***Aya* 1.** *Bismillaahi*. Sura zote za Qur'an - isipokuwa Baraa-at - zimeanza na *Bismillaahi*. Ibni Abbas anasimulia kuwa sura yo yote ilipoteremshwa, *Bismillaahi* ndiyo ilikuwa aya ya kwanza, na Mtume s.a.w. hakujua kuwa sura iliyoshuka ni mpya kama haikutanguliwa na *Bismillaahi.* (Abu Dawud). Hadithi hii inahakikisha kuwa *Bismillaahi* ni sehemu ya Qur'an hasa na ni sehemu ya sura zote zilizo nayo. Kadhalika kuna hadithi ya Mtume s.a.w. inayosema kuwa *Bismillaahi* ni sehemu ya sura zote za Qur'an (Bukhari na Kutni). Ile sura ya *Baraa-at* isiyo na *Bismillaahi* ni maendelezo tu ya sura Anfaal.

Mtume *s.a.w.* alisema ya kuwa kila kazi yenye maana inayoanzwa bila kusoma *Bismillaahi* hukosa kubarikiwa (Baidhawi). Hivyo Waislamu wamezoea kuanza kila kazi kwa *Bismillaahi.*

Sababu za kuanza *Bismillaahi* katika kila sura ya Qur'an ni hizi:-

1. Qur'an ni hazina ya elimu ya Kiungu ambayo mtu hawezi kuipata bila mapendeleo maalum ya Allah. Hivyo *Bismillaahi* imewekwa ili kumkumbusha msomaji ya kuwa anapotaka kuzifikia hazina za elimu iliyomo katika Qur'an aisome kwa nia safi, na mara kwa mara aombe msaada wa Allah, na aishi maisha ya kumcha Mungu.

2. Katika Agano la Kale (Kumbukumbu 18:18, 19) iliahidiwa kuwa atafika Mtume toka kwa ndugu za Waisraili (ambao ni watoto wa Ismail, nduguye Ishak aliyemzaa Israel) naye atawaambia watu maneno kwa jina la Mungu. Basi kwa kutimiza ufunuo huo Allah akajaalia kila sura ya Qur'an ianze na *Bismillaahi.* Hivyo aya hii kila inapoanza katika sura ya Qur'an inawakumbusha Mayahudi na Wakiristo kuwa ahadi ile imekwisha timia.

Aya 2. *Alhamdu lillaahi*. Mwislamu anafundishwa kusema; *Alhamdu lillaahi* (yaani, *sifa zote njema zinamhusu Allah*), na siyo kusema *Namsifu Mungu* au *Tunamsifu Mungu*. Kusema, "Sifa zote njema zinamhusu Allah" kuna maana kubwa zaidi kuliko kusema "Namsifu Mungu", kwa sababu mtu anaweza kumsifu Mungu sawa na elimu yake tu, lakini *Alhamdu lillaahi* (Sifa zote njema zinamhusu Allah) inakusanya sifa zile anazozijua mtu na pia zile asizozijua zilizo ni haki ya Allah.

Rabbil-'Alamiin, "Mola wa walimwengu." Neno *Rabb* lina maana ya Mola; Bwana; Mwenye kitu; Anayestahili kutiiwa; Anayetengeneza vilivyoharibika; Anayehifadhi na kukuza (Akrab na Lisan); Anayekamilisha kitu daraja hata daraja (Mufradat). Kadhalika *Rabb* maana yake ni Mwumbaji (Muhit). Po pote panapopatikana viumbe vya namna yo yote viwiliwili au roho, Mwumbaji na Mlezi wake ni Allah. Sifa hii ya Allah inaonyesha ya kwamba Mungu wa Uislamu si Mungu wa Waislamu peke yao, bali ni Mungu wa watu wote; ya kwamba dini hii ya Kiislamu haikuletwa kwa ajili ya kizazi au taifa fulani maalumu, bali kwa ajili ya Mataifa yote na kwa zama zote. Katika Mitume wote ni Mtume Muhammad saw peke yake aliyeanza kuwaita watu wote wa dunia washike dini aliyotumwa na Allah kuileta. Neno hili *Rabbil-'Aalamiin*

3. Mwingi wa rehema, Mwingi wa ukarimu,	الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ ۙ﴿٣﴾
4. Mmiliki wa siku ya malipo.	مٰلِكِ يَوْمِ الدِّيْنِ ؕ﴿٤﴾
5. Wewe tu twakuabudu, na Wewe tu twakuomba msaada.	اِيَّاكَ نَعْبُدُ وَ اِيَّاكَ نَسْتَعِيْنُ ؕ﴿٥﴾
6. Utuongoze kwenye njia iliyonyooka.	اِهْدِنَا الصِّرَاطَ الْمُسْتَقِيْمَ ۙ﴿٦﴾

pia linatujulisha ya kuwa sisi sote ni ndugu kwa kuwa Mwumba wetu ni Mmoja, na ya kuwa raha kamili haiji kwa mtu sharti wenziwe pia wawe na raha. Hivyo toka mwanzo tu Qur'an imefuta kabisa ubaguzi wa rangi na wa kabila, na kuwafanya wanadamu wote kuwa sawa. Fikira hii ingeshikwa, taabu nyingi na wasiwasi zilizoenea duniani zingekwisha

Aya 3. *Ar-Rahmaan,* "Mwingi wa rehema," ni neno linalotumika kwa ajili ya Allah tu. kama vile neno *Allah. Ar - Rahmaan* linadhihirisha sifa ile ya Allah ya kutoa vitu bure. Yaani aliweka tayari vitu vyote vinavyohitajiwa na viumbe kabla ya kuumbwa kwao, kama moto, maji, jua, vyakula na kadha wa kadha.

Ar-Rahiim, "Mwingi wa ukarimu," yaani Mungu atoaye malipo kwa ajili ya kila kazi na kila jitihada kwa kadiri inavyostahili. Juhudi za viumbe hazipotei bure naye hutoa malipo kwa kadiri ile ile inayostahili juhudi zao.

Aya 4. *Maaliki yaumi-d-Diin*, "Mmiliki wa siku ya Malipo." Kuna maneno matatu yanayofanana umbo lakini maana zake mbali mbali. Neno la hapa ni *Maalik* yaani "Mmiliki." Neno jingine ni *Malik* yaani "Mfalme"na jingine ni *Malak* yaani "Malaika."

Si mradi wa aya hii kwamba adhabu na thawabu zitakuwa siku ya Kiama tu, la, bali imebainishwa katika Qur'an mara kwa mara kuwa Kiama ni siku ya malipo makubwa; kwa hiyo katika dunia vile vile inaendelea namna ya adhabu na thawabu kama isemwavyo katika aya hii: *In tattaqullaaha yaj'allakum furqaanan,* yaani "Enyi mlioamini, mkimcha Allah atawajaalieni alama ipambanuayo" (sura 8:29). Tena Aya hii inaonyesha ya kuwa Allah ni Mmiliki, si kama vile watawala wa kidunia ambao kazi yao ni kutoa haki tu, bali Allah kwa kuwa yu Mmiliki anao uwezo wa kusamehe bila kutaka fidia. Hapa imebatilishwa imani ya Wakristo wanaodhani kuwa Mungu hangeweza kuwasamehe watu bure mpaka akalazimika kumtoa "mwanawe" Yesu auawe kuwa fidia ya dhambi za watu.

Aya 5. *Iyyaaka na'buduu.* "Wewe tu twakuabudu" . Neno la Kiarabu 'ibaada lina maana ya kutangaza umoja wa Allah, pia kumpenda kabisa, kutumainia kabisa, kumwogopa kabisa na kumnyenyekea kabisa. Tena ibada si kusali na kufunga tu, bali kila tendo jema linalofanywa kwa nia ya Kumpendeza Mungu, linakuwa ibada na linampatia mtu thawabu. Kwa kusema "twakuabudu" ambayo ni dhamiri ya wingi, Mwislamu anafundishwa ya kuwa mtu hakai peke yake duniani na ni lazima awe pamoja na wenzake katika mambo yote mema. Pili, mtu anapotaka salama asiwaachie wenziwe kupotea, afanye bidii kuwasuluhisha; kwani nyumba inayozungukwa na nyumba zingine zinazowaka moto haiwezi kuwa salama kwa muda mrefu.

Aya 6. *Ihdinaa.* "Utuongoze". Neno la Kiarabu *al-Hudaa* (Mwongozo) linatumika katika maana tatu: (1) kuonyesha njia iliyonyooka; (2) kuongoza kwenye njia iliyonyooka;

7. Njia ya wale Uliowaneemesha; ambao hawakughadhibikiwa na ambao hawakupotea.

صِرَاطَ الَّذِيْنَ اَنْعَمْتَ عَلَيْهِمْ ۙ غَيْرِ الْمَغْضُوْبِ عَلَيْهِمْ وَلَا الضَّآلِّيْنَ ۧ

(3) kumfanya mtu afuate siku zote njia iliyonyooka (Akrab, Mufradat na Baka). Na katika Qur'an neno hili limetumiwa katika maana zote hizo tatu katika aya hizi:(1) Sura 90 : 11; (2) Sura 29 : 70; (3) Sura 7 : 44. Dua hii ya ajabu si kama inatimiza mahitaji ya kiroho tu bali na ya kimwili pia. Mkristo amefundishwa kuomba apewe "siku kwa siku riziki" (Luka 11 : 3). Lakini Mwislamu amefunzwa kuomba dua inayokusanya mahitaji yake yote, ya kimwili na kiroho, ya sasa na ya baadaye pia.

Aya 7. *An'amta 'alaihim,* "Uliowaneemesha." Walioneemeshwa ambao Mwislam anafundishwa kuomba apewe neema zile walizopata wao, ni watu ambao wametajwa katika sura 4 : 70, yaani Manabii, Masiddik, Mashahidi, na Masalih (watu wema). Kadhalika katika sura 5 : 21 neema hizo zimesemwa kuwa ni Unabii na Ufalme. Aya hii inadhihirisha ya kuwa neema hizo zote zitaendelea kupatikana.

Manabii wataendelea kufika, Mawalii kadhalika, Mashahidi na Masalihi pia watafika. Hii ndiyo dalili inayohakikisha kuwa dini ya Kiislamu iko hai, na inaendelea kuangaliwa na Allah. Kufika kwa Seyidan Ahmad a.s. na kutangaza Utume wake uliothibitika kuwa sahihi na kudhihirika kwa Masiddik, Mashahidi na Watawa ni jambo linalozidi kuhakikisha kuwa Allah anaendelea kutimiza ahadi zake za kuilinda hii dini yake ya Kiislamu.

Sheikh Al-Amin bin Aly ameandika katika Tafsiri yake ya Juzu ya Alif Laam Miim, ukurasa wa nne, maelezo ya aya hii kama hivi: "Aya mbili hizi zatupa khabari ya watu waliotangulia kabla yetu na katika watu hao kuna ambao walikuwa wameshikamana na mambo mema, ambayo yatupasa nasi kushikamana nayo tupate ongoka kama walivyoongoka wao, na watu hao ni Mitume na watu wema aliowataja katika sura 4:68" (yaani sura 4:70).

Al-magh-dhuubi 'alaihim waladh-dhaalliin, "waliokasirikiwa wala ya (wale) waliopotea." Kwa kauli ya Mtume *s.a.w.*, "waliokasirikiwa" ni Mayahudi na "waliopotea" ni Wakristo (Tirmidhi na Musnad). Hapa Allah anawahadharisha Waislamu ya kuwa ingawa aya iliyotangulia imewaahidi baadhi yao kuwa watawarithi Manabii waliopita, kwa sababu ya ukweli wao na utukufu wao, na watapata neema za Unabii na Ujumbe, na neema zingine zilizotajwa; lakini pia kuna hatari ya baadhi yao kurithi sifa mbaya za Mayahudi kwa kukataa Mitume wao, na hivyo wapate adhabu duniani kama walivyopata Mayahudi. Na ya kwamba wengine watakaobaki watashika mila za Wakristo kwa vitendo na desturi zao. Basi hii ndiyo bishara iliyomo katika mwisho wa sura hii kwa mambo yatakayowafikia Waislamu katika hizi siku za mwisho.

Msomaji asiongozwe vibaya na neno *maghdhuubi* akadhani kwamba lina maana ya ile ghadhabu ya Allah tu waliyopata Mayahudi. Neno hili lina maana pana na linafunika siyo tu ile ghadhabu ya Allah bali pia ghadhabu ya watu ambayo wanaweza kuipata.

Ikumbukwe ya kuwa sura hii ni sehemu kubwa ya maneno yanayosomwa katika kila Sala, hata kila rakaa ya Sala. Mtume s.a.w. amesema; "Mtu aliyesali lakini hakusoma sura ya Alhamdu, basi Sala yake si kamili" (Muslim kitabu cha *Salaa*). Pia imesimuliwa na Ubada bin Samit ya kuwa Mtume s.a.w. alisema; "Asiyesoma sura ya Alhamdu katika sala, basi Sala yake si Sala" (Bukhari).

سُوْرَةُ الْبَقَرَةِ مَدَنِيَّةٌ وَّ هِيَ مَعَ الْبَسْمَلَةِ مِائَتَانِ وَ سَبْعٌ وَّ ثَمَانُوْنَ اٰيَةً وَّ اَرْبَعُوْنَ رُكُوْعًا

2. SURA AL-BAQARA

Imeteremshwa Madina

Ina mafungu 40 na Aya 287 pamoja na Bismillaahi

بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ ①

1. Kwa jina la Allah, Mwingi wa rehema, Mwingi wa ukarimu.

الٓمّٓ ②

2. Mimi ni Allah Nijuaye sana.

ذٰلِكَ الْكِتٰبُ لَا رَيْبَ ۛ فِيْهِ ۛ هُدًى لِّلْمُتَّقِيْنَ ③

3. Hicho ndicho Kitabu, kisicho na shaka yoyote ndani yake, ni mwongozo kwa wamchao (Allah).

Sura hii ilianza kuteremshwa katika mwaka wa kwanza baada ya Mtume s.a.w. kuhamia Madina na ikamalizika muda kidogo kabla Mtume hajafariki. Imeitwa Al-Baqara (Ng'ombe jike) yumkini kwa sababu ya habari ya ng'ombe aliyeabudiwa na Waisraeli iliyoelezwa ndani yake. Kadhalika sura hii inaitwa *Az-Zahraau* (Ing'aayo; nayo pamoja na sura *Aali 'Imraan* zimeitwa *Az-Zahraa-waan* (Mbili zing'aazo), (Muslim).

Aya 2-3. *Alif Laam Miim*. Herufi hizi, pamoja na herufi zingine zinazotokea mwanzo wa sura zingine 27, zinaitwa *Al-Muqatta'aat,* yaani, herufi zinazotamkwa mbalimbali. Desturi ya kutumia *Al-Muqatta'aat* ilikuwa imeenea katika Waarabu, nao walizitumia katika mashairi yao na katika mazungumzo yao. Siku hizi desturi hii imeenea sana duniani; na huku kwetu pia. Kwa mfano maneno haya: P.H.D., D.C., P.W.D., na mengineyo, hutumiwa sana.

Katika Qur'an herufi hizi zinaonyesha sifa maalum za Allah. Herufi hizi zinapowekwa mwanzo wa sura yo yote zinatoa habari mbele ya kuwa mambo yatakayoelezwa katika sura hiyo yanahusiana na sifa za Allah zinazosimamiwa na herufi hizo.

Ibni Abbas, aliyekuwa sahaba wa Mtume s.a.w., na aliyekuwa anajua sana elimu ya Qur'an, amesema ya kuwa maneno haya: *Alif, Laam, Miim*, maana yake ni *Anallaahu a'lamu* "Mimi ni Mungu Nijuaye sana" (Jarir). Kadhalika Seyyidna Ahmad (amani ya Mungu juu yake) amekubali tafsiri hiyo kwa kutoa sababu madhubuti za kuihakikisha. Kuna maana zingine pia za hizi *Muqatta'aat* lakini kubwa zaidi ni hiyo tuliyoitaja hapa.

Allah aliposema, *Mimi ni Mungu Nijuaye sana,* amehakikisha ya kuwa maneno yameteremshwa na Yeye mwenyewe ambaye ni Mjuzi wa tabia za wanadamu, na haja zao na kila wanalolihitaji. Hivyo akateremsha kitabu hiki kwa ujuzi ili kiwafaidie watu wa kila hali, wa kila upande na wa kila namna. Hiki si Kitabu kilichotungwa na Mtume Muhammad s.a.w. au Malaika; bali ni uteremsho halisi wa Allah Mwenye Kujua.

Katika Aya hizi mbili zilizo fupi sana Allah ameeleza Mambo yote yaliyo ya lazima kumtuliza mtu anayetaka kujua mbele kwa kifupi habari za Kitabu hiki. Mtu hutaka kujua mambo manne makubwa juu ya kitu cho chote: hutaka kujua (1) nani kakitengeneza, (2) ni kitu gani, (3) kakitengeneza namna gani, (4) kusudio la kitu hicho ni nini.

4. Ambao huyaamini yasiyo-onekana na husimamisha Sala na hutoa katika yale Tuliyowapa;

5. Na ambao wanaamini yali-yoteremshwa kwako na yaliyoteremshwa kabla yako, nao wana yakini na yale yatakayokuja baadaye.

الَّذِيْنَ يُؤْمِنُوْنَ بِالْغَيْبِ وَ يُقِيْمُوْنَ
الصَّلٰوةَ وَ مِمَّا رَزَقْنٰهُمْ يُنْفِقُوْنَ ۙ﴿۳﴾
وَالَّذِيْنَ يُؤْمِنُوْنَ بِمَآ اُنْزِلَ اِلَيْكَ
وَ مَآ اُنْزِلَ مِنْ قَبْلِكَ ۚ وَ بِالْاٰخِرَةِ
هُمْ يُوْقِنُوْنَ ؕ﴿۴﴾

Na mwanzoni tu Allah amejibu maswali hayo manne: (1) Nani kakitengeneza ? Amejibu, *Mimi Allah nijuaye sana.* (2) Ni kitu gani ? Amejibu, *Hicho ni Kitabu kamili* (*Al-Kitaabu* maana yake ni Kitabu kamili). (3) Kimetengenezwa namna gani ? *Hakina shaka (wala kosa) ndani yake.* (4) Kusudi lake nini? *Mwongozo kwa wamchao Mungu.*

Aya 4. *Ghaib*, "Yasiyoonekana" yaani, Allah, Malaika, Pepo, Jahannam na mengineyo. Pengine Aya hii imetafsiriwa, kuamini katika hali ya ghaibu na siri; yaani siyo kuonyesha imani mbele ya watu tu, hata kama mtu yu pembeni, atende kama itakavyo imani.

Husimamisha Sala, Allah hakusema *Na husali Sala,* bali amesema, *Na husimamisha Sala.* Kusimamisha Sala maana yake ni: (1) Mwislamu adumishe Sala maisha yake yote, akiangalia sana isimponyoke sala hata moja. (2) Asali mfululizo katika nyakati zilizowekwa, na asali sawa na sheria ya kusali. (3) Asali kwa roho moja, asijiachie mawazo yake kutangatanga ovyo na kuivuruga Sala yake. (4) Asali Sala zake kwa jamaa. (5) Awahimize watu wengine kusali mfululizo ili desturi ya kusali ienee.

Hutoa katika yale tuliyowapa, maana yake ni kwamba mcha Mungu anatakiwa atumie kwa kujifaidisha mwenyewe na kuwafaidisha viumbe wengine, kila kitu alichopewa na Allah, kama mali, akili, elimu, uwezo na vinginevyo. Katika Aya hii Allah ameonyesha ya kuwa dini ina makusudi mawili: kusudi la kwanza ni kutoa haki za Allah, yaani kumwabudu na kumshukuru. Sala inatimiza kusudi hili. Kusudi la pili ni kutoa haki za viumbe vyake.

Aya 5. Hapa Allah anatufunza ya kwamba mcha Mungu ni yule anayeamini maneno yake yaliyoteremshwa katika kila zama na kila nchi. Yaani, Waislamu wakubali kila ukweli uliopatikana kabla ya Uislamu, ukweli uliopo na utakaokuwepo baadaye. Maneno haya, *Na yaliyoteremshwa kabla yako,* yanaonyesha sifa maalum ya dini ya Kiislamu, yaani si kama Islam inakubali tu ukweli wa Mitume waliopita zamani, bali pia inawalazimisha Waislamu kuamini ya kuwa mafundisho ya Mitume hao yalitoka kwa Allah. Lakini ikumbukwe ya kuwa Islam ndio dini yenye mafundisho kamili tena ya mwisho, ambayo yamezidi uzuri mafundisho yote yaliyotangulia. Kwa hiyo kuamini mafundisho ya Mitume waliopita zamani, maana yake ni kuyaheshimu, sio kuyafuata na kuyatenda. Ndio maana katika Aya hii Allah ametanguliza kuamini Qur'an mbele kuliko kuamini Vitabu vya zamani, ambapo kwa kufuata mpango wa kufuatana, kuamini vitabu vya kale kungeliletwa mbele kuliko kuamini Qur'an. Na hii imepangwa hivyo kwa sababu waaminio watambue kuwa kuamini Vitabu vilivyotangulia kunategemea kuiamini Qur'an.

أُولٰٓئِكَ عَلٰى هُدًى مِّنْ رَّبِّهِمْ ۗ وَ أُولٰٓئِكَ هُمُ الْمُفْلِحُوْنَ ۝٥

6. Hao wako juu ya mwongozo utokao kwa Mola wao, na hao ndio wenye kufaulu.

اِنَّ الَّذِيْنَ كَفَرُوْا سَوَآءٌ عَلَيْهِمْ ءَاَنْذَرْتَهُمْ اَمْ لَمْ تُنْذِرْهُمْ لَا يُؤْمِنُوْنَ ۝٦

7. Hakika wale waliokufuru (ambao) ni sawa kwao uwaonye au usiwaonye, hawataamini.

خَتَمَ اللّٰهُ عَلٰى قُلُوْبِهِمْ وَعَلٰى سَمْعِهِمْ ۭ وَعَلٰٓى اَبْصَارِهِمْ غِشَاوَةٌ ۠ وَّلَهُمْ عَذَابٌ عَظِيْمٌ ۝٧

8. Allah Amepiga muhuri juu ya mioyo yao na juu ya masikio yao, na juu ya macho yao kuna kifuniko; na kwa ajili yao (imekadiriwa) adhabu kubwa.

FUNGU 2

وَمِنَ النَّاسِ مَنْ يَّقُوْلُ اٰمَنَّا بِاللّٰهِ وَبِالْيَوْمِ الْاٰخِرِ وَمَا هُمْ بِمُؤْمِنِيْنَ ۝٨

9. Na katika watu wako wasemao: Tumemwamini Allah na siku ya Mwisho; hali wao si wenye kuamini.

يُخٰدِعُوْنَ اللّٰهَ وَالَّذِيْنَ اٰمَنُوْا ۚ وَمَا يَخْدَعُوْنَ اِلَّآ اَنْفُسَهُمْ وَمَا يَشْعُرُوْنَ ۝٩

10. Wanajaribu kumdanganya Allah na wale walioamini, lakini hawadanganyi ila nafsi zao; nao hawatambui.

فِيْ قُلُوْبِهِمْ مَّرَضٌ ۙ فَزَادَهُمُ اللّٰهُ مَرَضًا ۚ وَلَهُمْ عَذَابٌ اَلِيْمٌ ۢ بِمَا كَانُوْا يَكْذِبُوْنَ ۝١٠

11. Mioyoni mwao mna maradhi, na Allah Amewazidishia maradhi; na kwa ajili yao (imekadiriwa) adhabu iumizayo kwa sababu walikuwa wakisema uwongo.

Aya 8. *Allah amepiga muhuri,* maana yake ni kuwa mtu anapoacha kutumia viungo vyake, muda mrefu ukipita vitalemaa. Kwa mfano, kama mtu ataendelea kukunja miguu yake siku zote bila kuikunjua, basi baadaye atashindwa kabisa kuikunjua - ndiyo adhabu yake aliyoisababisha yeye mwenyewe kwa kuacha kutumia vizuri miguu yake; namna hii wale makafiri ambao wanajionea ni sawa tu wakionywa au wasionywe , kwa sababu hawataki kutumia mioyo yao na masikio yao, wenyewe wanavilemaza na kuviharibu viungo vyao.

Aya 9. *Man yaquulu.* "Wako wasemao." Baada ya Allah kueleza habari za waaminio, na za makafiri, sasa zimeanza habari za wanafiki. Wanafiki ni wa namna mbili: (1) Watu ambao mioyoni hawana imani lakini wanajionyesha kwa waminio kuwa nao wanaamini, kwa sababu ya kutaka kujifaidisha na cho chote; (2) watu walioamini lakini hawana nguvu ya kuonyesha imani yao waziwazi.
Wanafiki wa namna ya (1) ndio wametajwa hapa. Na mfano wao umeelezwa katika Aya 18; na wanafiki wa namna ya pili mfano wao umeelezwa katika Aya 20. Mtume s.a.w. alieleza alama za mnafiki kuwa hizi: "Akizungumza anasema uwongo, akifunga ahadi haitimizi, akipewa amana anafanya hiyana; akifanya mapatano anavunja; akigombana anatoa matusi (Bukhari).

وَاِذَا قِيْلَ لَهُمْ لَا تُفْسِدُوْا فِى الْاَرْضِ ۙ قَالُوْٓا اِنَّمَا نَحْنُ مُصْلِحُوْنَ ⑫

12. Na wanapoambiwa, msifanye uharibifu ardhini, husema: Sisi ni wasuluhivu tu.

اَلَآ اِنَّهُمْ هُمُ الْمُفْسِدُوْنَ وَلٰكِنْ لَّا يَشْعُرُوْنَ ⑬

13. Zindukeni! Hakika wao ndio waharibifu, lakini hawatambui.

وَاِذَا قِيْلَ لَهُمْ اٰمِنُوْا كَمَآ اٰمَنَ النَّاسُ قَالُوْٓا اَنُؤْمِنُ كَمَآ اٰمَنَ السُّفَهَآءُ ۭ اَلَآ اِنَّهُمْ هُمُ السُّفَهَآءُ وَلٰكِنْ لَّا يَعْلَمُوْنَ ⑭

14. Na wanapoambiwa: Aminini kama walivyoamini watu, husema: Je, tuamini kama walivyoamini wapumbavu? Fahamuni! Hakika wao ndio wapumbavu lakini hawajui.

وَاِذَا لَقُوا الَّذِيْنَ اٰمَنُوْا قَالُوْٓا اٰمَنَّا ۚ وَاِذَا خَلَوْا اِلٰى شَيٰطِيْنِهِمْ ۙ قَالُوْٓا اِنَّا مَعَكُمْ ۙ اِنَّمَا نَحْنُ مُسْتَهْزِءُوْنَ ⑮

15. Na wanapokutana na walioamini husema: Tumeamini; na wanapokuwa peke yao kwa mashetani wao, husema: Hakika sisi tu pamoja nanyi; sisi tunawafanyia tu dhihaka.

اَللّٰهُ يَسْتَهْزِئُ بِهِمْ وَيَمُدُّهُمْ فِىْ طُغْيَانِهِمْ يَعْمَهُوْنَ ⑯

16. Allah Atawalipa tu dhihaka yao na kuwaacha katika upotevu wakitangatanga ovyo.

اُولٰٓئِكَ الَّذِيْنَ اشْتَرَوُا الضَّلٰلَةَ بِالْهُدٰى ۠ فَمَا رَبِحَتْ تِّجَارَتُهُمْ وَمَا كَانُوْا مُهْتَدِيْنَ ⑰

17. Hao ndio walionunua upotevu kwa uongofu; lakini biashara yao haikupata faida, wala hawakuweza kuwa wenye kuongoka.

Aya 15. *Shayaatiinihim,* "Mashetani wao," yaani wakubwa wa uasi miongoni mwa makafiri na wanafiki waliokuwa wakijivuna waliotajwa katika sura 33:68.

Aya 17. *Walionunua upotevu kwa uongofu.* Maneno haya mradi wake ni (1) wameacha mwongozo na badala yake wameshika upotevu; au (2) vyote viwili, mwongozo na upotevu, walivipewa lakini wakachagua upotevu na kukataa mwongozo. Maana hizi mbili zote zinakubalika hapa. Maana ya kwanza inaonyesha ya kwamba mwanadamu kwa asili yake ni mtu safi na ana vipawa vilivyo bora (sura 30:31; na 95:5), lakini kwa kupewa mafunzo mabaya au kwa kutenda mabaya tabia yake safi ya asili inapotea. Hivyo "uongofu" hapa mradi wake ni ile tabia ya asili ambayo kila mtu amepewa na Allah na kwa kuitumia vibaya anaipoteza na anapotea. Na maana ya pili ni kwamba Allah huwatuma Mitume pamoja na mwongozo, na upande mwingine Shetani anawaletea watu upotevu. Hapo watu wabaya wanachagua upotevu wa Shetani na wanapotea.

Padre Dale ameandika juu ya Aya hii na akasema, "Muhammad alifanya biashara, ndio maana alipenda kutumia maneno ya biashara hapa na penginepo" (uk. 544 wa Tafsiri yake). Maneno haya kwa hakika ameyaandika ili kushawishi ya kwamba Qur'an ni utungo tu wa Mtume Muhammad s.a.w. Lakini hii si kweli. Kwanza Padre Dale hangeweza kusema kuwa Allah asingeweza kusema maneno hayo. Kutumia usemi wa namna hii ni fasaha inayofikisha

مَثَلُهُمْ كَمَثَلِ الَّذِي اسْتَوْقَدَ نَارًا ۚ فَلَمَّآ
اَضَآءَتْ مَا حَوْلَهٗ ذَهَبَ اللّٰهُ بِنُوْرِهِمْ
وَتَرَكَهُمْ فِيْ ظُلُمٰتٍ لَّا يُبْصِرُوْنَ ﴿١٧﴾

18. Mfano wao ni kama mfano wa yule aliyekoka moto, na ulipoyaangaza yaliyo pembezoni mwake, Allah Akaiondoa nuru yao na kuwaacha katika giza, hawaoni.

صُمٌّۢ بُكْمٌ عُمْيٌ فَهُمْ لَا يَرْجِعُوْنَ ﴿١٨﴾ لا

19. Ni viziwi, mabubu, vipofu; kwa hiyo hawatarejea (kwenye mwongozo).

اَوْ كَصَيِّبٍ مِّنَ السَّمَآءِ فِيْهِ ظُلُمٰتٌ
وَّرَعْدٌ وَّبَرْقٌ ۚ يَجْعَلُوْنَ اَصَابِعَهُمْ فِيْٓ
اٰذَانِهِمْ مِّنَ الصَّوَاعِقِ حَذَرَ الْمَوْتِ ؕ
وَاللّٰهُ مُحِيْطٌۢ بِالْكٰفِرِيْنَ ﴿١٩﴾

20. Na (mfano wao) ni kama mvua kubwa itokayo mawinguni, ndani yake mna giza na radi na umeme; hutia vidole vyao masikioni mwao kutokana na ngurumo kwa kuogopa kufa; na Allah ni Mwenye kuwazunguka makafiri.

يَكَادُ الْبَرْقُ يَخْطَفُ اَبْصَارَهُمْ ؕ كُلَّمَآ
اَضَآءَ لَهُمْ مَّشَوْا فِيْهِ ۙ وَاِذَآ اَظْلَمَ

21. Ni karibu umeme unyakue kuona kwao; kila unapowaangazia

---

jambo mara moja katika moyo wa mtu. Ni wazi ya kuwa kumweleza mkulima jambo au kumweleza mwashi au seremala, huelewa vizuri anapoelezwa kwa mfano wa jambo analoshughulika nalo sana. Na "kununua" ni jambo ambalo karibu kila mtu duniani analifanya; na hivyo badala ya kutumia mfano kama wa "mpandaji" mbegu aliotumia Yesu (Mat. 8:5-8) ambao unaweza kufahamiwa vizuri zaidi na wakulima tu, si na wachungaji, Qur'an imetumia mfano wa "kununua" unaoweza kufahamiwa chapu chapu na kila mtu.

Zaidi ya hayo Qur'an imeeleza mara kwa mara juu ya kuumbwa viumbe na madaraja mbalimbali ya kuumbwa kwao. Je, Padre Dale atasema hayo yamesemwa kwa sababu Mtume *s.a.w.* alikuwa akiumba? Habari za ujenzi, uhunzi, safari za mabahari na mambo mbalimbali kadha wa kadha yameelezwa katika Qur'an. Je, Padre Dale atasema Mtume s.a.w. alikuwa nahodha au mwashi au mhunzi?

Katika Luka 5:37 Yesu anasema, "Wala hakuna mtu atiaye divai mpya katika viriba vikuukuu; na kama akitia, ile divai mpya itavipasua vile viriba, divai yenyewe itamwagika, na viriba vitaharibika. Lakini divai mpya sharti kutiwa viriba vipya. Wala hakuna anywaye divai ya kale, akatamani divai mpya; kwa kuwa asema, ile ya kale ndiyo iliyo njema." Divai ni mvinyo au tuseme pombe ya zabibu. Kwa kufuata falsafa ya Padre Dale, maneno haya ya Yesu yataonyesha ya kwamba alifanya kazi ya kupika pombe, bali alikuwa akiinywa na alikuwa mlevi; maana Padre Dale anaweza kuhoji ya kuwa habari za pombe na namna ya kuitengeneza na kuihifadhi na ladha yake zingemkaaje kichwani?

Aya 19. Aya hii yaweza kuhusiana na kundi la wanafiki wanaoelezwa kuwa ni viziwi, mabubu na vipofu kwa sababu ya msimamo wao wa kutokusikiliza ukweli, kutokusema ukweli wala kuona ukweli. Kwa hiyo wao kwa hiari yao wamezikana hekima za busara zao na wakajifungia kwa ndani.

Aya 21. *Al-Barqu,* "Umeme" Hapa umeme mradi wake ni nguvu ya Uislamu iliyokuwa ikijitokeza mara kwa mara na kuwatia tamaa hao wanafiki waliokuwa dhaifu katika imani; lakini mara nguvu ile ikimalizika kidogo basi nao wanaanza tena kubabaika.

عَلَيْهِمْ قَامُوْا ۭ وَلَوْ شَاۗءَ اللّٰهُ لَذَهَبَ
بِسَمْعِهِمْ وَاَبْصَارِهِمْ ۭ اِنَّ اللّٰهَ عَلٰي
كُلِّ شَيْءٍ قَدِيْرٌ ۝٢٠ ع ٢

(kuwaonyesha njia) hutembea ndani yake; na linapowawia giza, husimama; na kama Allah Angependa bila shaka Angaliondoa kusikia kwao na kuona kwao; hakika Allah ni Mwenye uwezo juu ya kila kitu.

FUNGU 3

يٰٓاَيُّهَا النَّاسُ اعْبُدُوْا رَبَّكُمُ الَّذِيْ خَلَقَكُمْ
وَالَّذِيْنَ مِنْ قَبْلِكُمْ لَعَلَّكُمْ تَتَّقُوْنَ ۝٢١ ۙ

22. Enyi watu! Mwabuduni Mola wenu Ambaye amewaumba ninyi na wale wa kabla yenu ili mpate ucha Mungu.

الَّذِيْ جَعَلَ لَكُمُ الْاَرْضَ فِرَاشًا وَّالسَّمَاۗءَ
بِنَاۗءً ۠ وَّاَنْزَلَ مِنَ السَّمَاۗءِ مَاۗءً فَاَخْرَجَ بِهٖ
مِنَ الثَّمَرٰتِ رِزْقًا لَّكُمْ ۚ فَلَا تَجْعَلُوْا لِلّٰهِ
اَنْدَادًا وَّاَنْتُمْ تَعْلَمُوْنَ ۝٢٢

23. Ambaye Amewafanyieni ardhi kuwa tandiko na mbingu kuwa paa, na Akateremsha maji kutoka mawinguni na kwayo Akatoa matunda ya kila namna yawe riziki kwenu; basi msimfanyizie Allah washirika na hali ninyi mnajua.

وَاِنْ كُنْتُمْ فِيْ رَيْبٍ مِّمَّا نَزَّلْنَا عَلٰي عَبْدِنَا
فَاْتُوْا بِسُوْرَةٍ مِّنْ مِّثْلِهٖ ۠ وَادْعُوْا
شُهَدَاۗءَكُمْ مِّنْ دُوْنِ اللّٰهِ اِنْ كُنْتُمْ
صٰدِقِيْنَ ۝٢٣

24. Na ikiwa mna shaka kwa hayo Tuliyomteremshia Mtumishi wetu, basi leteni sura iliyo mfano wa hii, na mwaite wasaidizi wenu ghairi ya Allah ikiwa mnasema kweli.

فَاِنْ لَّمْ تَفْعَلُوْا وَلَنْ تَفْعَلُوْا فَاتَّقُوا
النَّارَ الَّتِيْ وَقُوْدُهَا النَّاسُ وَالْحِجَارَةُ ۚ
اُعِدَّتْ لِلْكٰفِرِيْنَ ۝٢٤

25. Lakini kama hamtafanya, na hamtafanya kamwe, basi uogopeni moto ambao kuni zake ni watu na mawe, ulio-andaliwa makafiri.

Aya 24. *Fa'tuu bisuuratin min mithlihii.* "Leteni sura iliyo mfano wa hii." Hapa wasio-amini wanaambiwa kuwa kama Qur'an haifai kuaminiwa, na kama haikutoka kwa Allah, basi nao walete sura yenye sifa za Qur'an; maana kazi inayofanywa na mwanadamu inaweza kufanywa na mwanadamu mwingine. Lakini kama kazi imefanywa na Allah, basi hakuna mtu anayeweza kuifanya. Mpaka leo wasioamini wameshindwa katika jambo hili na inathibitika ya kuwa Kitabu hiki hakikutungwa na ye yote isipokuwa Allah Mwenyewe.

Aya 25. *Fattaqunaara.* "Basi uogopeni Moto" Ingawa moto na mawe vimetajwa, isid-haniwe vitu hivyo ni hasa namna ya hivi tulivyo navyo. Vimefanana majina tu. Maisha ya Akhera si ya kimwili kama haya; ni ya kiroho na vitu vyake pia ni vya kiroho, na vyenye nguvu zaidi.

وَبَشِّرِ الَّذِيْنَ اٰمَنُوْا وَعَمِلُوا الصّٰلِحٰتِ اَنَّ
لَهُمْ جَنّٰتٍ تَجْرِيْ مِنْ تَحْتِهَا الْاَنْهٰرُ ؕ
كُلَّمَا رُزِقُوْا مِنْهَا مِنْ ثَمَرَةٍ رِّزْقًا ۙ قَالُوْا
هٰذَا الَّذِيْ رُزِقْنَا مِنْ قَبْلُ ۙ وَاُتُوْا بِهٖ
مُتَشَابِهًا ؕ وَلَهُمْ فِيْهَآ اَزْوَاجٌ مُّطَهَّرَةٌ ۙ
وَّهُمْ فِيْهَا خٰلِدُوْنَ ﴿٢٥﴾

26. Na wabashirie walioamini na kufanya vitendo vizuri, kwamba watapata Mabustani ipitayo mito ndani yake; kila mara watakapopewa matunda humo kuwa riziki, watasema: Haya ndiyo tuliyopewa zamani, ilhali hapo kabla waliletewa tu (riziki) iliyofanana na hiyo; na humo watapata wenzi waliotakaswa, nao watakaa humo milele.

اِنَّ اللّٰهَ لَا يَسْتَحْيٖٓ اَنْ يَّضْرِبَ مَثَلًا مَّا
بَعُوْضَةً فَمَا فَوْقَهَا ؕ فَاَمَّا الَّذِيْنَ اٰمَنُوْا
فَيَعْلَمُوْنَ اَنَّهُ الْحَقُّ مِنْ رَّبِّهِمْ ۚ وَاَمَّا
الَّذِيْنَ كَفَرُوْا فَيَقُوْلُوْنَ مَاذَآ اَرَادَ اللّٰهُ
بِهٰذَا مَثَلًا ۘ يُضِلُّ بِهٖ كَثِيْرًا ۙ وَّيَهْدِيْ بِهٖ
كَثِيْرًا ؕ وَمَا يُضِلُّ بِهٖٓ اِلَّا الْفٰسِقِيْنَ ﴿٢٦﴾

27. Hakika Allah haoni haya kutoa mfano wo wote hata kama ni wa mbu na ulio juu yake. Ama waaminio, basi wanajua ya kwamba hiyo ni haki iliyotoka kwa Mola wao; lakini wale waliokufuru husema: Ni nini analotaka Allah kwa mfano huu? Huwapoteza wengi kwa huo na Huwaongoza wengi kwa huo; lakini Hapotezi ye yote kwa (mfano) huo isipokuwa wavunjao amri,

الَّذِيْنَ يَنْقُضُوْنَ عَهْدَ اللّٰهِ مِنْۢ بَعْدِ مِيْثَاقِهٖ ۠
وَيَقْطَعُوْنَ مَآ اَمَرَ اللّٰهُ بِهٖٓ اَنْ يُّوْصَلَ
وَيُفْسِدُوْنَ فِي الْاَرْضِ ؕ اُولٰٓئِكَ هُمُ
الْخٰسِرُوْنَ ﴿٢٧﴾

28. Ambao wanavunja ahadi ya Allah baada ya kuifunga na huyakata Aliyoamrisha Allah kuunganishwa na hufanya ufisadi katika ardhi; hao ndio wenye hasara.

كَيْفَ تَكْفُرُوْنَ بِاللّٰهِ وَكُنْتُمْ اَمْوَاتًا
فَاَحْيَاكُمْ ۚ ثُمَّ يُمِيْتُكُمْ ثُمَّ يُحْيِيْكُمْ
ثُمَّ اِلَيْهِ تُرْجَعُوْنَ ﴿٢٨﴾

29. Mtamkataaje Allah na hali mlikuwa wafu naye Akawahuisheni, kisha Atawafisheni, kisha Atawahuisheni, kisha Kwake mtarejeshwa.

Aya 26. *Walioamini na kufanya vitendo vizuri.* Pepo ya Kiislamu inaahidiwa wale waliochanganya mambo mawili: Imani na vitendo vyema. Imani bila vitendo vyema ni kama bustani isiyopita maji; na vitendo vyema bila imani ni kama maji matupu bila bustani.

Haya ndiyo tuliyopewa zamani. Mradi wake ni matunda ya kiroho ambayo watu watawa wanayaonja bado wangali hapa hapa duniani. *Tuliyopewa* inaweza pia kutafsiriwa, *Tuliyoahidiwa* na Aya ikasomeka hivi: *Haya ndiyo tuliyoahidiwa zamani.*

Wataletewa yafananayo, yaani matendo ya ibada wanayofanya waaminio hapa duniani yatafanana na matunda watakayopewa Peponi.

30. Yeye ndiye Aliyewaumbieni vyote vilivyomo katika ardhi, kisha Akaelekea kwenye mbingu na Akazisawazisha katika sura ya mbingu saba, naye ndiye Ajuaye kila kitu.

هُوَ الَّذِیۡ خَلَقَ لَکُمۡ مَّا فِی الۡاَرۡضِ
جَمِیۡعًا ۚ ثُمَّ اسۡتَوٰۤی اِلَی السَّمَآءِ فَسَوّٰىهُنَّ
سَبۡعَ سَمٰوٰتٍ ؕ وَ هُوَ بِکُلِّ شَیۡءٍ عَلِیۡمٌ ﴿۲۹﴾

FUNGU 4

31. Na (kumbuka) Mola wako Alipowaambia Malaika: Hakika Mimi nataka kumteua Khalifa katika ardhi; wakasema: Je, Utamweka humo atakayefanya uharibifu humo na kumwaga damu, hali sisi twakutukuza kwa sifa Zako na kukutaja utakatifu wako? Akasema: Hakika Mimi Nayajua msiyoyajua.

وَ اِذۡ قَالَ رَبُّکَ لِلۡمَلٰٓئِکَۃِ اِنِّیۡ جَاعِلٌ
فِی الۡاَرۡضِ خَلِیۡفَۃً ؕ قَالُوۡۤا اَتَجۡعَلُ فِیۡهَا
مَنۡ یُّفۡسِدُ فِیۡهَا وَ یَسۡفِکُ الدِّمَآءَ ۚ
وَ نَحۡنُ نُسَبِّحُ بِحَمۡدِکَ وَ نُقَدِّسُ لَکَ ؕ
قَالَ اِنِّیۡۤ اَعۡلَمُ مَا لَا تَعۡلَمُوۡنَ ﴿۳۰﴾

Aya 30. *Aliyewaumbieni vyote vilivyomo katika ardhi.* Katika sura 45:14 Allah Amesema, "Na Amewatiishieni vilivyomo mbinguni na ardhini ..... " Fundisho hili linatufunza tujifaidishe na vitu vyote vilivyomo duniani na mbinguni. Huu ndio msingi wa elimu zote. Aya hizi zinashuhudia ukamilifu wa Qur'an. Vitu vilivyodhaniwa zamani kuwa havifai pole pole vinavumbuliwa manufaa yao makubwa.

Aya 31. *Mimi nitamweka Khalifa katika ardhi.* Maneno haya ni kinyume na hadithi za watu wanaosema, Adamu aliwekwa mbinguni. Neno Khalifa lina maana tatu: (1) mtu anayekuja baadaye kushika mahali pa mtu aliyekuwepo; (2) Imam, yaani Kiongozi mkubwa wa dini; (3) Sultani, mfalme au mtawala (Akrab). Maana hizo zinadhihirisha kuwa walikuwepo watu kabla ya kuzaliwa Adamu, na yeye alitumwa kuwa Mjumbe wa Allah kwa watu hao.

Adamu aliyeishi miaka 6,000 iliyopita anafahamiwa kwa shangwe sana kuwa ndiye mtu wa kwanza kabisa kuumbwa na Mungu duniani. Hakika ni hii ya kuwa dunia hii imepita katika maduara namna mbalimbali ya viumbe na ustaarabu. Fikira hii pia imeshikwa na Walii mkuu wa Kiislamu aitwaye Muhyi-d-Din Ibni Arabi, ambaye anasema ya kwamba safari moja aliona katika ndoto akiizunguka Kaaba. Katika ndoto hiyo mtu akamtokea na akamwambia kuwa yeye ni mmoja wa babu zake. Ibni Arabi akamwuliza, "Ni miaka mingapi toka ulipokufa?" Yule mtu akamjibu, "Zaidi kuliko miaka elfu arobaini." Ibni Arabi akajibu, "Lakini muda huu ni mkubwa kuliko ule unaotutenga na Adamu." Mtu yule akamwuliza, "Unasema Adamu gani? Adamu huyu wa karibu yenu au mwingine?" Ibni Arabi anasema, "Hapo nilikumbuka Hadithi ya Mtume s.a.w. isemayo kwamba Allah alileta ma-Adamu wasiopungua mia moja elfu, na nikajiambia, 'Labda huyu mtu anayesema ni babu yangu ni mmoja katika ma-Adamu waliopita zamani'" (Futuuhat, Jalada iii, 607).

Kadhalika neno Khalifa analoitwa Adamu linaonyesha ya kwamba alikuwa ni mmoja katika mabaki ya watu wa zamani na akachaguliwa na Allah kuanzisha taifa jipya.

Hatukubaliani na Biblia inayosema kuwa mtu wa kwanza kuumbwa duniani ni Adamu. Mbali na ushahidi unaoletwa, historia huonyesha kuwa kulikuwa na watu miaka mingi mno kabla ya

وَعَلَّمَ اٰدَمَ الْاَسْمَآءَ كُلَّهَا ثُمَّ عَرَضَهُمْ
عَلَى الْمَلٰٓئِكَةِ ۙ فَقَالَ اَنْۢبِـُٔوْنِيْ بِاَسْمَآءِ
هٰٓؤُلَآءِ اِنْ كُنْتُمْ صٰدِقِيْنَ ﴿٣٢﴾

32. Na Akamfundisha Adamu Majina yote, kisha Akawaweka (viumbe wale) mbele ya Malaika, na Akasema: Niambieni majina ya hawa ikiwa mwasema kweli.

قَالُوْا سُبْحٰنَكَ لَا عِلْمَ لَنَآ اِلَّا مَا
عَلَّمْتَنَا ؕ اِنَّكَ اَنْتَ الْعَلِيْمُ الْحَكِيْمُ ﴿٣٣﴾

33. Wakasema: Utakatifu ni Wako! Hatuna elimu isipokuwa Uliyotufundisha; bila shaka Wewe ndiwe Mjuzi, Mwenye hekima.

قَالَ يٰٓاٰدَمُ اَنْۢبِئْهُمْ بِاَسْمَآئِهِمْ ۚ
فَلَمَّآ اَنْۢبَاَهُمْ بِاَسْمَآئِهِمْ ۙ قَالَ اَلَمْ
اَقُلْ لَّكُمْ اِنِّيْٓ اَعْلَمُ غَيْبَ السَّمٰوٰتِ
وَ الْاَرْضِ ۙ وَ اَعْلَمُ مَا تُبْدُوْنَ
وَمَا كُنْتُمْ تَكْتُمُوْنَ ﴿٣٤﴾

34. Akasema Ewe Adamu, waambie majina yao; basi alipowaambia majina yao, Akasema: Je, Sikuwaambieni kwamba Mimi Naijua siri ya mbingu na ya ardhi na Nayajua mnayoyadhihirisha na mnayoyaficha?

وَاِذْ قُلْنَا لِلْمَلٰٓئِكَةِ اسْجُدُوْا لِاٰدَمَ

35. Na (kumbukeni) Tulipowaambia Malaika: Mtiini Adamu، na wakatii wote

---

Adamu, hata Biblia yenyewe haikusimama imara juu ya jambo hili. Kwa mfano toka mlango wa nne wa Kitabu cha Mwanzo, tunaonyeshwa ya kwamba Adamu alizaa watoto wawili, Kain na Habil, na Kain alimwua nduguye, kisha akaondoka kwenda kaa nchi ya Nod, na akaoa huko. Swali ni hili: yule mkewe alitoka wapi? Nchi ya Nod ilikujaje, na ni watu gani alioogopa wasije mwua hata ikalazimu atiwe alama, kama ni kweli hakukuwa watu wengine ila Adamu na mkewe na watoto wao wawili tu ndio waliokuwapo?

Kadhalika si maoni yetu kwamba watu wote walioenea pande zote za dunia ni wazao wa Adamu yule yule mmoja. Bali tunashika ya kwamba Adamu huyu hakuwa mtu wa kwanza. Watu walikuwako kabla yake. Kwa hiyo hatuwezi kusema kama wenyeji wa asili wa Amerika, Australia na kwingineko ni wazao wa Adamu huyu au Adamu mwingine.

Aya 32. *Majina.* Mradi wake ni Majina ya Allah (tazama sura 7:181). Maulamaa wamehitilafiana hapa. Wengine wanasema majina hayo ni majina ya vitu: yaani alifundishwa lugha; na wengine wanasema ni majina ya watoto wake.

'Aradhwahum. "Akawaweka." Maulamaa wengine wamefasiri neno hili "Akaviweka" yaani vitu. Lakini neno "hum" si dhamiri (kijina) ya vitu kwa kanuni za lugha ya Kiarabu. Lingekuwa ni dhamiri ya vitu neno hilo lingekuwa *'Aradhwahaa.* Hivyo kufasiri "Akawaweka" kama tulivyofanya ndiyo sawa.

Aya 34. *Mnayoyadhihirisha na mnayoyaficha*. Ndiyo kusema ya kwamba Allah anajua ni sifa Zake gani Malaika wanazoweza kuzibainisha, na ni zipi wasizoweza kuzibainisha. Sio mradi wake kuwa Malaika walimficha Allah cho chote. Umbile la kibinadamu lina uwezo wa kudhihirisha sifa zaidi za Allah kuliko umbile la kimalaika. Huu ndio mradi wa Aya hii.

Aya 35. *Isjuduu li Aadama.* "Mtiini Adamu." Neno sajada (kusujudu) kwa Kiarabu lina maana hizi: (1) kunyenyekea; (2) kuinama; (3) kusujudu (Akrab); (4) kutii na kuabudu (Mufradat). Si sawa kufasiri, "Msujudieni Adamu," maana imekatazwa kusujudia cho chote isipokuwa Allah (41:38)·

فَسَجَدُوْٓا اِلَّآ اِبْلِيْسَ ؕ اَبٰى وَاسْتَكْبَرَ ۫ وَكَانَ مِنَ الْكٰفِرِيْنَ ﴿٣٤﴾

isipokuwa Ibilisi - alikataa na akafanya kiburi; naye alikuwa ni miongoni mwa makafiri.

وَقُلْنَا يٰٓاٰدَمُ اسْكُنْ اَنْتَ وَزَوْجُكَ الْجَنَّةَ وَكُلَا مِنْهَا رَغَدًا حَيْثُ شِئْتُمَا ۪ وَلَا تَقْرَبَا هٰذِهِ الشَّجَرَةَ فَتَكُوْنَا مِنَ الظّٰلِمِيْنَ ﴿٣٥﴾

36. Na Tulisema: Ewe Adamu, kaa wewe na mkeo katika bustani, na kuleni humo kwa maridhawa po pote mpendapo, lakini msiukaribie mti huu waila mtakuwa miongoni mwa wadhalimu.

فَاَزَلَّهُمَا الشَّيْطٰنُ عَنْهَا فَاَخْرَجَهُمَا مِمَّا كَانَا فِيْهِ ۪ وَقُلْنَا اهْبِطُوْا بَعْضُكُمْ لِبَعْضٍ عَدُوٌّ ۚ وَلَكُمْ فِى الْاَرْضِ مُسْتَقَرٌّ وَّمَتَاعٌ اِلٰى حِيْنٍ ﴿٣٦﴾

37. Basi Shetani akawatelezesha humo wote wawili katika suala la mti ule na akawatoa mle walimokuwemo hapo awali. Ndipo Tukawaambia: tokeni, m maadui ninyi kwa ninyi, na (imekadiriwa kuwa) mtakaa na kunufaika katika ardhi hii hadi muda fulani.

فَتَلَقّٰٓى اٰدَمُ مِنْ رَّبِّهٖ كَلِمٰتٍ فَتَابَ عَلَيْهِ ؕ اِنَّهٗ هُوَ التَّوَّابُ الرَّحِيْمُ ﴿٣٧﴾

38. Basi Adamu akajifunza maneno fulani (ya maombi) kwa Mola wake, naye Akapokea toba yake; hakika Yeye ndiye Apokeaye toba, Mwingi wa ukarimu.

Ibliis. Yeye hakuwa Malaika; maana Allah anasema, *Malaika 'hawamwasi Allah Ali-yowaamuru, na hutenda wanayoamrishwa"* (66:7); lakini Ibilisi aliasi, hivyo hakuwa Malaika. Katika Aya hii Allah amefupisha maneno na inaonekana Ibilisi kana kwamba alikuwa mmoja wa Malaika. Lakini katika sura 7:13 Allah anaonyesha kuwa Ibilisi pia alipewa amri ya kumtumikia Adamu lakini hakutii, ndipo Allah akamkasirikia.

Ibilisi ni mbali na Shetani aliyempoteza Adamu. Qur'an yenyewe inawapambanua. Kila inaposimulia juu ya yule aliyekataa kumtii Adamu inamtaja Ibilisi; na kila inapomweleza yule aliyempoteza Adamu inamtaja Shetani. Sura 18:51 inaeleza kuwa Ibilisi alikuwa miongoni mwa *jinn* (viumbe wa siri) ambao, kinyume na *Malaika,* wao walipewa uwezo wa kutii na kuasi.

Aya 36. *Jannat*. Hapa neno hili maana yake si Pepo, bali ni bustani ya hapa duniani, maana sura 15:49 inasema ya kuwa mara mtu akiingia Peponi hatoki milele, hali Adamu alitolewa katika jannat (bustani) aliyokuwemo. Uchunguzi wa siku hizi umebainisha ya kuwa mahali alipowekwa Adamu ni katika bustani ya Eden iliyokuwa karibu na Babelon katika nchi ya Irak au Assyria.

Shajarah. "Mti." Kwa Kiarabu neno hili lina maana hizi zingine: ugomvi, na jadi ya mtu (Lane). Yumkini Adamu alikatazwa kuingia katika magomvi, na mambo mabaya. Biblia inasema ulikuwa mti wa kujua mema na mabaya (Mwanzo 2:17), yaani mti wa elimu. Haiyumkini Allah akamkataza mtu kupata ujuzi ambao huo tu ndio unaweza kumfanya awe mtu. Na kama Adamu alikosa hali hajui yepi mema na yepi mabaya, Allah asingalimlaumu.

قُلْنَا اهْبِطُوْا مِنْهَا جَمِيْعًا ۚ فَاِمَّا يَاْتِيَنَّكُمْ
مِّنِّيْ هُدًى فَمَنْ تَبِعَ هُدَايَ فَلَا خَوْفٌ
عَلَيْهِمْ وَلَا هُمْ يَحْزَنُوْنَ ﴿٣٩﴾
وَالَّذِيْنَ كَفَرُوْا وَكَذَّبُوْا بِاٰيٰتِنَآ اُولٰٓئِكَ
اَصْحٰبُ النَّارِ ۚ هُمْ فِيْهَا خٰلِدُوْنَ ﴿٤٠﴾ ع

39. Tukasema: Tokeni humo nyote; na kama ukiwafikieni mwongozo utokao Kwangu basi watakaofuata mwongozo Wangu, basi haitakuwa hofu juu yao wala hawatahuzunika.

40. Lakini wenye kukufuru na kuzikadhibisha Ishara Zetu, hao ndio watu wa Motoni, watakaa humo kwa muda mrefu.

FUNGU 5

يٰبَنِيْٓ اِسْرَآءِيْلَ اذْكُرُوْا نِعْمَتِيَ الَّتِيْٓ
اَنْعَمْتُ عَلَيْكُمْ وَاَوْفُوْا بِعَهْدِيْٓ اُوْفِ
بِعَهْدِكُمْ ۚ وَاِيَّايَ فَارْهَبُوْنِ ﴿٤١﴾

41. Enyi wana wa Israeli, ikumbukeni neema Yangu Niliyowaneemesheni, na itekelezeni ahadi Yangu, Nitatekeleza ahadi yenu; na Niogopeni Mimi tu.

وَاٰمِنُوْا بِمَآ اَنْزَلْتُ مُصَدِّقًا لِّمَا مَعَكُمْ
وَلَا تَكُوْنُوْٓا اَوَّلَ كَافِرٍ بِهٖ ۠ وَلَا تَشْتَرُوْا
بِاٰيٰتِيْ ثَمَنًا قَلِيْلًا ۠ وَّاِيَّايَ فَاتَّقُوْنِ ﴿٤٢﴾

42. Na aminini Niliyoyateremsha, yasadikishayo yaliyo pamoja nanyi, wala msiwe wa kwanza kuyakataa. Wala msiziuze Ishara Zangu kwa thamani ndogo; na Nicheni Mimi tu.

Aya 41. *Israaiil* ni jina jingine la Nabii Yakubu bin Nabii Is'hak. Jina hili alipewa na Allah baadaye (Mwanzo 32:28). Neno hili maana yake ni (1) Sultani wa Mungu; (2) Mpiganaji vita wa Mungu; (3) Askari wa Mungu. Kadhalika neno hili linatumiwa katika maana mbalimbali: (1) Yakubu mwenyewe anaitwa *Israil* (Mwanzo 32:28); (2) wazao wake wanaitwa *Israil* (Kumbukumbu ya Torati 6:3,4); mtu au watu wo wote wacha Mungu wanaitwa *Israil* (Heb. - Eng. Lexicon).

Aya 42. *Musaddiqan*. "Yasadikishayo." Tamko hili linapotumiwa kwa Mitume au Vitabu vilivyopita linaweza kuonyesha mambo matatu: (1) Madai ya Mtume na Vitabu vilivyotangulia kuwa vimetoka kwa Allah ni kweli; (2) Kwamba mafundisho waliyotoa ni ya haki; (3) Kutimiza bishara zilizoelezwa juu ya kufika Mtume baadaye, au kushuka ufunuo baadaye, n.k.w.

Katika Aya hii neno *musaddiqan* limetumiwa kwa maana hii ya tatu. Kila mara Qur'an inapojisema ni *musaddiqan li* au *lahu* kama lilivyo hapa, haina maana ya kwamba inakubali usahihi wa mafundisho ya Vitabu hivyo, ila tu ya kwamba inasadikisha bishara zilizotajwa katika Vitabu hivyo kwa kuzitimiza.

Haiwezekani kusema ya kwamba Qur'an inaona mafundisho ya Vitabu hivyo vyote ni sahihi, maana Vitabu hivyo vyenyewe vina mafundisho yanayohitilafiana na kadhalika mafundisho ya Qur'an yenyewe yanahitilafiana na mafundisho ya Vitabu vya dini hizo. Hivyo Qur'an haingeweza kusadikisha kwamba mafundisho ya Vitabu inayohitilafiana navyo ni sahihi; maana mengi katika Vitabu vya zamani yameharibiwa na mengine mengi yalikuwa yamekusudiwa kwa nyakati zao maalum tu.

43. Na msichanganye haki na batili wala msifiche haki na hali mnajua.

وَلَا تَلْبِسُوا الْحَقَّ بِالْبَاطِلِ وَتَكْتُمُوا الْحَقَّ وَاَنْتُمْ تَعْلَمُوْنَ ﴿٤٢﴾

44. Na simamisheni Sala na toeni Zaka na inameni pamoja na wainamao.

وَاَقِيْمُوا الصَّلٰوةَ وَاٰتُوا الزَّكٰوةَ وَارْكَعُوْا مَعَ الرّٰكِعِيْنَ ﴿٤٣﴾

45. Je, mnawaamuru watu kutenda mema na mnajisahau nafsi zenu hali mnasoma Kitabu, basi je, hamtumii akili?

اَتَاْمُرُوْنَ النَّاسَ بِالْبِرِّ وَتَنْسَوْنَ اَنْفُسَكُمْ وَاَنْتُمْ تَتْلُوْنَ الْكِتٰبَ ؕ اَفَلَا تَعْقِلُوْنَ ﴿٤٤﴾

46. Na ombeni msaada kwa subira na kwa Sala; na kwa hakika jambo hilo ni gumu isipokuwa kwa wanyenyekevu.

وَاسْتَعِيْنُوْا بِالصَّبْرِ وَالصَّلٰوةِ ؕ وَاِنَّهَا لَكَبِيْرَةٌ اِلَّا عَلَى الْخٰشِعِيْنَ ۙ﴿٤٥﴾

47. Ambao wana yakini ya kwamba watakutana na Mola wao na ya kwamba watarejea kwake.

الَّذِيْنَ يَظُنُّوْنَ اَنَّهُمْ مُّلٰقُوْا رَبِّهِمْ وَاَنَّهُمْ اِلَيْهِ رٰجِعُوْنَ ﴿٤٦﴾ ع

Wakristo hudhani ya kuwa Aya hii inaonyesha mafundisho ya Vitabu vyao ni sahihi. Labda wanadhani hivyo kwa kukosa kujua Kiarabu vizuri, maana Aya hiyo na zingine kama hiyo hazina mradi wa hayo wanayoyataka.

Kama neno hilo *musaddiqan* lingekuwa na maana ya kusadikisha kitu kuwa ni sahihi na kukifuata, neno hilo lingesomeka *musaddiqan* tu au *musaddiqan bi.*

Ajabu ni hii ya kuwa Bwana Yesu alisema, "Msidhani kama nimekuja kutangua sheria au Manabii, sikuja kutangua bali kutimiza" (Matei 5:17). Lakini juu ya hayo hawafuati mafundisho ya sheria na Manabii, yaliyomo katika Agano la Kale. Na Qur'an inayosema kuwa imekuja kutangua Vitabu na baadhi ya sheria zilizopita zamani, (sura 2:107) wao wanapenda waone ndani yake kuwa inakiri usahihi wa mafundisho yao!

Aya 43. Qur'an inaonyesha makosa yasiyopungua matatu ya wana wa Israeli yanayohusiana na Biblia: (1) Kuchanganya haki na batili, (2) kuficha haki na (3) kubadili maneno (sura 2:76).

Padre Dale na wengineo wanajaribu sana kutaka kuonyesha kuwa Qur'an inasadikisha Vitabu vya Biblia kuwa viko katika hali ile ile vilivyokuwa nayo zamani. Lakini Qur'an, mbali na kusadikisha wazo hilo, inaling'oa na mizizi yake.

Kila mtu anayejishughulisha na Vitabu vya Wakristo anajua, na mapadre pia wanajua kuwa wanabadilisha Vitabu vyao mara kwa mara. Kwa mfano Injili iliyopigwa chapa mwaka 1945, Waraka wa Yuda 1:14 imesema, "Na Enok, wa saba baada ya Adamu, alitoa maneno ya Unabii juu ya hao, akisema, Angalia, Bwana alikuja na *elfu kumi za watakatifu wake"*. Bishara hii inaonyesha kufika kwa Bwana, yaani Mtume Muhammad s.a.w., pamoja na watakatifu elfu kumi. Nayo ilitimia wakati Mtume s.a.w. alipoishinda Makka pamoja na Masahaba wake elfu kumi.

Bishara hii tuliieleza mara kwa mara tukiwakaribisha Wakristo wampokee Nabii waliyeahidiwa ambaye bishara hiyo imemtimilia. Sasa mapadre wameona kuwa maneno hayo ni hatari kwa ajili yao; hivyo katika Injili iliyopigwa chapa mwaka 1950 maneno yale wameyabadili, na sasa ile hesabu elfu kumi ya watakatifu walioandamana na Mtume Muhammad s.a.w. haionekani. Wameyabadili hivi; "Na Henoko, mtu wa saba baada ya Adamu, alitoa maneno ya Unabii juu ya hao, akisema, Angalia, Bwana alikuja na *watakatifu wake maelf maelf."* (Union Version). Kadhalika Injili iliyopigwa chapa kwa lugha ya Kijaluo hata neno elfu halipatikani; wameandika hivi, *"Gogendini mage*

FUNGU 6

يٰبَنِيۡۤ اِسۡرَآءِيۡلَ اذۡكُرُوۡا نِعۡمَتِىَ الَّتِىۡۤ اَنۡعَمۡتُ عَلَيۡكُمۡ وَاَنِّىۡ فَضَّلۡتُكُمۡ عَلَى الۡعٰلَمِيۡنَ ﴿۴۸﴾

48. Enyi wana wa Israeli! Kumbukeni neema Yangu Niliyowaneemesheni na Nikawapeni fadhila juu ya viumbe wote.

وَاتَّقُوۡا يَوۡمًا لَّا تَجۡزِىۡ نَفۡسٌ عَنۡ نَّفۡسٍ شَيۡـًٔا وَّلَا يُقۡبَلُ مِنۡهَا شَفَاعَةٌ وَّلَا يُؤۡخَذُ مِنۡهَا عَدۡلٌ وَّلَا هُمۡ يُنۡصَرُوۡنَ ﴿۴۹﴾

49. Na iogopeni siku ambayo nafsi haitaifaa nafsi nyingine cho chote, wala hayatakubaliwa kwake maombezi, wala haitapokewa fidia kwake; wala hawatasaidiwa.

وَاِذۡ نَجَّيۡنٰكُمۡ مِّنۡ اٰلِ فِرۡعَوۡنَ يَسُوۡمُوۡنَكُمۡ سُوۡٓءَ الۡعَذَابِ يُذَبِّحُوۡنَ اَبۡنَآءَكُمۡ وَيَسۡتَحۡيُوۡنَ نِسَآءَكُمۡ ؕ وَفِىۡ ذٰلِكُمۡ بَلَآءٌ مِّنۡ رَّبِّكُمۡ عَظِيۡمٌ ﴿۵۰﴾

50. Na (kumbukeni) Tulipowaokoeni kwa watu wa Firauni, waliowapeni adhabu mbaya, wakiwachinja wavulana wenu na kuwaacha hai wanawake wenu, na katika hayo lilikuwamo jaribio kubwa kutoka kwa Mola wenu.

وَاِذۡ فَرَقۡنَا بِكُمُ الۡبَحۡرَ فَاَنۡجَيۡنٰكُمۡ وَاَغۡرَقۡنَاۤ اٰلَ فِرۡعَوۡنَ وَاَنۡتُمۡ تَنۡظُرُوۡنَ ﴿۵۱﴾

51. Na (kumbukeni) Tulipoitenga bahari kwa ajili yenu na Tukawaokoeni, na Tukawazamisha watu wa Firauni na hali mkitazama.

---

maler" yaani "Na makundi yake matakatifu." Siyo kwamba lugha ya Kijaluo haina neno la "elfu" ambalo ni "gana" au "eluf," bali ni kwa sababu maneno hayo *elfu kumi* yanasaidia kuhakikisha ukweli wa Mtume Muhammad *s.a.w*. na dini ya Kiislamu, hivyo, bila kumwogopa Allah wameyabadilisha.

Kadhalika Injili ya mwaka 1945 (Mattayo 10:23) inasema, "Hamtaimaliza miji *yote* ya Israeli hata ajapo mwana wa Adamu."Injili ya mwaka 1950 inasema, "Hamtaimaliza miji ya Israeli." Neno *yote* hapo limekwisha ondolewa. Na Injili ya Kijaluo haina kabisa neno *Israeli*. Humo imeandikwa hivi, *Ok unutiek limo mier duto ngang'* yaani, "Hamtamaliza kutazama miji yote." Yaani, sasa si miji ya Israeli tu bali ni *miji yote.* Yote hii ni juhudi inayofanywa pole pole kubadilisha "Vitabu vyao vya Mungu" kidogo kidogo. Neno "Israeli" wameliondoa maana likiwepo itathibitika kuwa bishara aliyotoa Yesu ya kufika kwake mara ya pili haikuwa kweli.

Na kama ni kweli wanavyodai Wakristo ya kuwa Injili zao ziliandikwa kwa uwezo wa Roho Mtakatifu, na haya maneno mawili "yote" na "Israeli" hapo mwanzo pia yaliandikwa humo kwa uwezo wa Roho Mtakatifu, je sasa Roho Mtakatifu ameyaghairi kwa sababu gani.?

Isitoshe wao hupenyeza maneno katika Vitabu vyao pia. Injili ya mwaka 1945, Yohana 1:18 inasema, *"Mwana wa pekee* aliye katika kifua cha Baba." Lakini Injili iliyotangazwa mwaka 1950 imeongeza neno jingine na kubadilisha kabisa maana iliyokuwapo toka zamani. Hiyo inasema hivi,*"Mungu Mwana* pekee aliye katika kifua cha Baba."

Ikiwa katika zama hizi za nuru mapadre wanathubutu kufanya ujasiri wa kuyaingilia kwa fujo maneno wanayosadiki kuwa ni ya Allah, basi imebaki juu ya msomaji kufikiri mwenyewe zama hizo za giza na ujahili kazi hii waliiendesha kwa kiasi gani!

وَاِذْ وٰعَدْنَا مُوْسٰٓى اَرْبَعِيْنَ لَيْلَةً ثُمَّ اتَّخَذْتُمُ الْعِجْلَ مِنْۢ بَعْدِهٖ وَاَنْتُمْ ظٰلِمُوْنَ ﴿٥٢﴾

52. Na (kumbukeni) Tulipomwahidi Musa siku arobaini, kisha mkamshika ndama (kuwa mungu) baada (ya kuondoka kwake) na mkawa wadhalimu.

ثُمَّ عَفَوْنَا عَنْكُمْ مِّنْۢ بَعْدِ ذٰلِكَ لَعَلَّكُمْ تَشْكُرُوْنَ ﴿٥٣﴾

53. Kisha Tukawasameheni baada ya hayo ili mpate kushukuru.

وَاِذْ اٰتَيْنَا مُوْسَى الْكِتٰبَ وَالْفُرْقَانَ لَعَلَّكُمْ تَهْتَدُوْنَ ﴿٥٤﴾

54. Na (kumbukeni) Tulipompa Musa Kitabu na Ishara zipambanuazo ili mpate kuongoka.

وَاِذْ قَالَ مُوْسٰى لِقَوْمِهٖ يٰقَوْمِ اِنَّكُمْ ظَلَمْتُمْ اَنْفُسَكُمْ بِاتِّخَاذِكُمُ الْعِجْلَ فَتُوْبُوْٓا اِلٰى بَارِئِكُمْ فَاقْتُلُوْٓا اَنْفُسَكُمْ ؕ ذٰلِكُمْ خَيْرٌ لَّكُمْ عِنْدَ بَارِئِكُمْ ؕ فَتَابَ عَلَيْكُمْ ؕ اِنَّهٗ هُوَ التَّوَّابُ الرَّحِيْمُ ﴿٥٥﴾

55. Na (kumbukeni) Musa alipowaambia watu wake; Enyi watu wangu, hakika ninyi mmejidhulumu nafsi zenu kwa kushika ndama (kuwa mungu)! Basi tubuni kwa Mwumba wenu na ziueni nafsi zenu; hayo ni bora kwenu mbele ya Mwumba wenu; basi Akapokea toba yenu, hakika Yeye ndiye apokeaye toba, Mwingi wa Ukarimu.

وَاِذْ قُلْتُمْ يٰمُوْسٰى لَنْ نُّؤْمِنَ لَكَ حَتّٰى نَرَى اللّٰهَ جَهْرَةً فَاَخَذَتْكُمُ الصّٰعِقَةُ وَاَنْتُمْ تَنْظُرُوْنَ ﴿٥٦﴾

56. Na (kumbukeni) mliposema: Ewe Musa hatutakuamini kamwe mpaka tumwone Allah waziwazi! Ndipo ikawashikeni ngurumo na hali mnaona!

ثُمَّ بَعَثْنٰكُمْ مِّنْۢ بَعْدِ مَوْتِكُمْ لَعَلَّكُمْ تَشْكُرُوْنَ ﴿٥٧﴾

57. Kisha Tukawafufueni baada ya (hali yenu ya) umauti, ili mpate kushukuru.

Aya 57. *Tukawafufueni baada ya kufa kwenu.* Au yaweza kutafsiriwa; Kisha Tukawafufueni baada ya (hali yenu inayofanana na) umauti, ili mpate kushukuru. Sasa ni kifo gani walichokufa? Je roho zilitoka kabisa miilini? Ndiyo maswali yaliyopita na yanapita ndani ya vichwa vya wanaotafakari. Upande mmoja wanaona Qur'an imesema wanaokufa hawarudi duniani (sura 21:96). Hapo wanajihoji ilikuwaje hawa wakafufuka hapa hapa duniani? Je, Qur'an imekuwa kigeugeu, sasa iseme hivi na baadaye iseme vingine?

Hakika ni hii ya kuwa, siyo kama Qur'an ina maneno yanayopinzana, bali neno *maut* (kifo) kwa lugha ya Kiarabu, sio kila siku huwa na maana ya kutoka roho. Neno hili lina maana nyingi, kama (1) kukoma uwezo wa kukua (sura 50:12). (2) Kutokwa na fahamu (sura 19:24). (3) Kukosa akili (sura 6:123). (4) Kulemewa na huzuni, sikitiko au hofu (sura 14:18). (5) Kutokwa na Ucha Mungu au kufa kiroho. (sura 3:170). (6) Usingizi ambao Waarabu wanauita kifo chepesi (Mufradat). (7) Kutulia kimya. (8) Kuwa maskini. (9) Kuchakaa. (10) Kudhalilika, kuwa duni, kudharaulika, kuwa hafifu na mnyonge kabisa. (11) Mji kukosa wakazi, au shamba kukosa kulimwa (Lane). Kadhalika "Lisaan" kinaeleza *maut* (mauti) kwa maana kama hizo. Hivyo kifo kilichotajwa katika Aya hii ni ama kifo cha kiroho kwa kutomtii Allah au huzuni kubwa au hofu iliyowafikia kwa sababu ya adhabu ya kutisha waliyopewa. Pia tazama sura 3:50.

وَظَلَّلْنَا عَلَيْكُمُ الْغَمَامَ وَاَنْزَلْنَا عَلَيْكُمُ
الْمَنَّ وَالسَّلْوٰى ؕ كُلُوْا مِنْ طَيِّبٰتِ مَا
رَزَقْنٰكُمْ ؕ وَمَا ظَلَمُوْنَا وَلٰكِنْ كَانُوْٓا
اَنْفُسَهُمْ يَظْلِمُوْنَ ﴿٥٧﴾

58. Na Tukawatilieni kivuli kwa mawingu na Tukawateremshieni Manna na Salwa: Kuleni katika vitu safi Tulivyowaruzukuni. Nao hawakutudhulumu, lakini walikuwa wamejidhulumu nafsi zao.

وَاِذْ قُلْنَا ادْخُلُوْا هٰذِهِ الْقَرْيَةَ فَكُلُوْا مِنْهَا
حَيْثُ شِئْتُمْ رَغَدًا وَّ ادْخُلُوا الْبَابَ
سُجَّدًا وَّ قُوْلُوْا حِطَّةٌ نَّغْفِرْ لَكُمْ
خَطٰيٰكُمْ ؕ وَسَنَزِيْدُ الْمُحْسِنِيْنَ ﴿٥٨﴾

59. Na (kumbukeni) Tuliposema: Ingieni kijiji hiki, na humo kuleni kwa maridhawa po pote mpendapo, na ingieni katika mlango kwa kutii, na semeni; Tusamehe dhambi zetu, Tutawasameheni makosa yenu, na Tutawazidishia wafanyao hisani.

فَبَدَّلَ الَّذِيْنَ ظَلَمُوْا قَوْلًا غَيْرَ الَّذِيْ قِيْلَ
لَهُمْ فَاَنْزَلْنَا عَلَى الَّذِيْنَ ظَلَمُوْا رِجْزًا
مِّنَ السَّمَآءِ بِمَا كَانُوْا يَفْسُقُوْنَ ﴿٥٩﴾ ع

60. Lakini waliodhulumu wakabadili kauli ghairi ya ile waliyoambiwa, kwa hiyo Tukaiteremsha juu ya wale waliodhulumu, adhabu kutoka mbinguni, kwa sababu walikuwa wakiasi.

FUNGU 7

وَاِذِ اسْتَسْقٰى مُوْسٰى لِقَوْمِهٖ فَقُلْنَا
اضْرِبْ بِّعَصَاكَ الْحَجَرَ ؕ فَانْفَجَرَتْ
مِنْهُ اثْنَتَا عَشْرَةَ عَيْنًا ؕ قَدْ عَلِمَ كُلُّ اُنَاسٍ
مَّشْرَبَهُمْ ؕ كُلُوْا وَاشْرَبُوْا مِنْ رِّزْقِ اللّٰهِ
وَلَا تَعْثَوْا فِى الْاَرْضِ مُفْسِدِيْنَ ﴿٦٠﴾

61. Na (kumbukeni) Musa alipoomba maji kwa ajili ya watu wake, ndipo Tukasema: Lipige jiwe kwa fimbo yako; mara zikabubujika humo chemchem kumi na mbili; kila kabila likajua mahala pao pa kunywea: Kuleni na kunyweni katika riziki ya Allah, wala msiasi katika ardhi mkifanya uharibifu.

Aya 58. *Kivuli kwa mawingu.* Huko jangwani walikokuwa kulikuwa na shida ya kivuli, maji na chakula. Mawingu yaliwateremshia mvua na pia kuwatia kivuli. *Manna* maana yake ni (1) kitu anachopewa mtu kwa hisani; (2) kitu cho chote kinachopatikana bila taabu wala shida; (3) kitu fulani kitamu kinachoshuka kama umande *(honeydew)* (Akrab). *Sal'wa* ni (1) ndege mweupe-mweupe anayefanana na tombo (namna ya kware) anayepatikana katika sehemu za Bara Arabu na ujiranini mwake; (2) cho chote kinachomfanya mtu atosheke na afurahi; (3) asali (Akrab).

Aya 61. *Lipige jiwe kwa fimbo yako.* Huu ni mmojapo katika miujiza ya Nabii Musa; Allah alimjulisha jiwe hasa lililokuwa likipita maji chini yake; na mara alipolipiga maji yakatoka.

62. Na (kumbukeni) mliposema: Ewe Musa, hatutaweza kusubiri juu ya chakula cha namna moja, basi tuombee kwa Mola wako Atutolee katika vile inavyoviotesha ardhi - kama mboga zake na matango yake na ngano yake na adesi zake na vitunguu vyake. Akasema: Je, mnataka kubadili vitu hafifu kwa vile vilivyo bora? Nendeni kwenye mji na kwa yakini huko mtapata mlivyoviomba; na ikapigwa juu yao dhila na umaskini, nao wakarudi na ghadhabu ya Allah: Hayo ni kwa sababu walikuwa wakizikataa Ishara za Allah na wakajaribu kuwaua Manabii pasipo haki; hayo ni kwa sababu waliasi na walikuwa wakiruka mipaka.

وَاِذْ قُلْتُمْ يٰمُوْسٰى لَنْ نَّصْبِرَ عَلٰى
طَعَامٍ وَّاحِدٍ فَادْعُ لَنَا رَبَّكَ يُخْرِجْ
لَنَا مِمَّا تُنْۢبِتُ الْاَرْضُ مِنْۢ بَقْلِهَا
وَقِثَّآئِهَا وَفُوْمِهَا وَعَدَسِهَا وَبَصَلِهَا ؕ
قَالَ اَتَسْتَبْدِلُوْنَ الَّذِىْ هُوَ اَدْنٰى
بِالَّذِىْ هُوَ خَيْرٌ ؕ اِهْبِطُوْا مِصْرًا فَاِنَّ
لَكُمْ مَّا سَاَلْتُمْ ؕ وَضُرِبَتْ عَلَيْهِمُ
الذِّلَّةُ وَالْمَسْكَنَةُ ۗ وَبَآءُوْ بِغَضَبٍ
مِّنَ اللّٰهِ ؕ ذٰلِكَ بِاَنَّهُمْ كَانُوْا يَكْفُرُوْنَ
بِاٰيٰتِ اللّٰهِ وَيَقْتُلُوْنَ النَّبِيّٖنَ بِغَيْرِ الْحَقِّ ؕ
ذٰلِكَ بِمَا عَصَوْا وَّكَانُوْا يَعْتَدُوْنَ ﴿٦١﴾ ع

Chemchem kumi na mbili. Padre Dale anadhani kuwa Qur'an imekosea habari za maji ya Horeb na kuchanganya na habari za visima kumi na mbili vya Elim. Kwa hakika yeye mwenyewe ndiye amekosea, kwa kudhani ya kuwa maadamu Biblia (Kutoka 17:1-7; Hesabu 20:2-11) imetaja habari ya jiwe lililopigwa na Musa na yakatoka maji, bali haitaji ni mifereji mingapi iliyotoka, basi hapo anafikiri labda ni kuchanganya na habari za visima kumi na mbili vya Elim.

Ni wazi hapa ya kwamba ingawa Biblia haikutaja hesabu ya chemchem zile, kama ambavyo haitaji baadhi ya habari zilizo sahihi zinazoelezwa na Qur'an, Qur'an imesema jambo la kweli kabisa ambalo linakubaliwa hata na adui mwingine wa Uislamu, George Sale. Yeye anasema katika ukurasa wa tisa wa tafsiri yake maneno haya, "Jiwe hilo limesimama mipakani mwa Bara Arabu na baadhi ya wana-nchi wenziwe lazima walikuwa wameliona ikiwa yeye mwenyewe hakuliona, kama ilivyo yumkini kabisa kwamba naye pia aliliona. Na kwa hakika anaonekana hakukosa. Maana mtu ambaye alikwenda pande hizo mwishoni mwa karne ya kumi na tano anatuambia dhahiri ya kwamba maji yalitiririka katika mahala kumi na mbili pa jiwe hilo sawa na idadi ya makabila ya Waisraeli."

Ni yumkini kabisa ya kwamba Padre Dale amesoma maelezo hayo ya Sale yanayohakikisha usahihi wa maelezo ya Qur'an juu ya chemchem hizo kumi na mbili. Lakini, ama kwa sababu ya uadui alio nao juu ya Uislamu, au kwa sababu ya kuchelea kudhihirisha upungufu wa Biblia iliyoacha kutaja idadi ya mifereji hiyo, ameona afadhali apuuze maelezo yenye ushahidi ulio wazi yaliyotolewa na Sale, kisha alete lawama ya bure juu ya Qur'an na kutafuta kuitetea Biblia pasina haki.

Aya 62. *Atutolee katika vile inavyoviotesha ardhi.* Waliomba washike maisha ya ukulima na hali Allah alitaka wakae maisha ya jangwani wakila wanyama wa pori na mboga za pori, ili mioyo yao itoke woga, na wapate ujasiri, wawe tayari kuitawala nchi ya Kanaan waliyoahidiwa. Maombi yao yanaonyesha hawakuziamini ahadi za Allah; hivyo akawakasirikia, wakaruhusiwa kukaa mjini, na huko wakadhalilika.

FUNGU 8

63. Hakika waaminio na Mayahudi na Wakristo na Wasabii (wenye kuamini vitabu vingine vya kimbingu), ye yote miongoni mwao atakayemwamini Allah na siku ya mwisho na kufanya vitendo vizuri, basi watapata ujira wao kwa Mola wao, wala haitakuwa hofu juu yao, wala hawatahuzunika.

إِنَّ الَّذِينَ آمَنُوا وَالَّذِينَ هَادُوا وَالنَّصَارَىٰ
وَالصَّابِئِينَ مَنْ آمَنَ بِاللَّهِ وَالْيَوْمِ الْآخِرِ
وَعَمِلَ صَالِحًا فَلَهُمْ أَجْرُهُمْ عِنْدَ رَبِّهِمْ
وَلَا خَوْفٌ عَلَيْهِمْ وَلَا هُمْ يَحْزَنُونَ ﴿٦٢﴾

Aya 63. *Wasabii.* Wasabii ni jina walilopewa watu wa namna nne: (1) Watu waliokuwa wakiabudu nyota walioishi katika nchi ya Mesopotamia (Gibbon's *Roman Empire,* Vol. v, pp. 440: na *Muruuj adh-Dhahab* kilichotungwa na Mas'uudi; na Enc. Rel. Eth. viii, katika habari za Mandoeans). (2) Dini iliyokuwa mchanganyiko wa Kiyahudi, Kikristo na kizarishti (Kathir, chini ya sura 2:63). (3) Watu walioishi karibu na Mosul katika nchi ya Iraq ambao waliamini Mungu lakini hawakuwa na Kitabu cha sheria kinachojulikana. Walidai ya kuwa walikuwa wanafuata dini ya Nabii Nuhu (Jarir na Kathir, chini ya sura 2:63). Watu walioishi karibu na Iraq waliosema ya kuwa wanaamini Manabii wote wa Allah na walikuwa na desturi maalum ya kusali na kufunga saumu (Kathir). Baadhi ya Mafukahaa wa Kiislamu waliwahesabu Wasabii kuwa ni Watu wa Kitabu.

Hapa Allah ametaja nguzo kubwa mbili, ya kwanza na ya mwisho, na nguzo zingine zote za Uislamu zinaingia ndani yake. Yaani mwenye kumwamini Allah na Siku ya Mwisho lazima ataamini Mitume wote, na Vitabu vyote na Malaika na uwezo wa Allah.

Sio mradi hapa kuwa hata Wasabii, Wayahudi na Wakristo nao wako salama kwa dini hizo. Sura 4:151, 152 na sura 6:93 zinaonyesha waziwazi kuwa kuamini Allah na Siku ya Mwisho ni kuamini Qur'an na Mitume wote. Hivyo Wasabii na Mayahudi na Wakristo kwa mujibu wa Aya hii si wenye kumwamini Allah na Siku ya Mwisho kweli kweli; basi hawatapata salama.

Katika Aya hii imeonyeshwa ya kuwa alipofika Mtume *s.a.w.* dini zingine tatu zilikuwa katika uwanja wa mashindano. Hivyo, kama vile siku za Nabii Musa, maadui zake ndio walishindwa na dini yake ya haki ikastawi, na kama vile katika siku za Nabii Isa dini zingine baadaye zilififia na dini yake ya haki ikastawi, kadhalika dini ya Mtume Muhammad *s.a.w.* kwa kuwa ndiyo ya haki, ilibidi ifanikiwe na zingine zishindwe. Mafanikio ya ajabu ya Uislamu yaliyowaangusha washinde wote hao yalithibitisha kuwa Waislamu ndio hasa waliomwamini Allah na Siku ya Mwisho. Maanguko ya leo ya Waislamu yalitabiriwa zamani na Mtume Muhammad *s.a.w.* kuwa yatatokea kwa sababu Waislamu wataacha kuzingatia barabara maagizo ya Uislamu. Kadhalika mafanikio ya Mataifa ya Wakristo leo ambayo hayakuja kwa sababu ya kufuata dini yao, pia yalitabiriwa na Mtume *s.a.w.* na kutimia kwake kunazidi kuhakikisha ukweli wa dini ya Kiislamu. Tukumbuke ya kuwa Mtume *s.a.w.* pia alitabiri ya kuwa Uislamu utainuka tena katika kufika kwa Masihi Aliyeahidiwa. Kufika kwa Seyyidna Ahmad, mwanzo wa karne hii ya 14 ya Hijra kuwa Masihi aliyeahidiwa, kumeanzisha tena kazi ya kuuimarisha Uislamu na kuupa mafanikio ya kabisa mpaka mwisho, na dini ya Kiislamu anayoibashiri yeye na wafuasi wake ndiyo itakayoshinda na kutukuka duniani.

وَاِذْ اَخَذْنَا مِيْثَاقَكُمْ وَرَفَعْنَا فَوْقَكُمُ
الطُّوْرَ ؕ خُذُوْا مَآ اٰتَيْنٰكُمْ بِقُوَّةٍ
وَّاذْكُرُوْا مَا فِيْهِ لَعَلَّكُمْ تَتَّقُوْنَ ﴿٦٣﴾

64. Na (kumbukeni) Tulipotwaa ahadi yenu na Tukaunyanyua mlima juu yenu: Shikeni kwa nguvu Tuliyowapeni na yakumbukeni yaliyomo ili mpate kumcha Mungu.

ثُمَّ تَوَلَّيْتُمْ مِّنْۢ بَعْدِ ذٰلِكَ ۚ فَلَوْلَا فَضْلُ
اللّٰهِ عَلَيْكُمْ وَرَحْمَتُهٗ لَكُنْتُمْ مِّنَ
الْخٰسِرِيْنَ ﴿٦٤﴾

65. Kisha mligeuka baada ya hayo; na kama isingekuwa fadhili za Allah juu yenu na rehema Zake, bila shaka mngalikuwa miongoni mwa wenye hasara.

وَلَقَدْ عَلِمْتُمُ الَّذِيْنَ اعْتَدَوْا مِنْكُمْ فِي
السَّبْتِ فَقُلْنَا لَهُمْ كُوْنُوْا قِرَدَةً خٰسِئِيْنَ ﴿٦٥﴾

66. Na kwa yakini mmekwisha wajua wale walioasi miongoni mwenu katika (amri ya) Sabato. Basi tukawaambia: Kuweni manyani wadhalilifu.

Aya 64. *Tuur,* "Mlima." Neno hili lina maana ya (1) mlima au kilima; (2) mlima Turi au Sinai (Mufradat na Akrab. Maneno haya: *Tukaunyanyua mlima juu yenu,* sio mradi wake ya kuwa mlima Sinai ulinyanyuliwa ukaelea hewani juu ya vichwa vya Waisraeli. Maana yake, ahadi hiyo ilifungwa walipokuwa chini ya mlima ambako Allah aliwaamrisha waende wakasimame. Kanuni ya lugha ya Kiarabu inaruhusu maneno kutumika hivyo kwa kutoa maana hii tunayoieleza.

Aya 66. Mayahudi walipewa adhabu hii kwa sababu, Allah alipotaka watumie siku ya Jumamosi kuwa Sabato yao, na wajifurahishe katika mambo ya kidini tu bila kujiingiza katika mambo ya kidunia, wao hawakutii amri hiyo, wakaendelea na kazi zingine zisizokuwa za dini. Kwa mwendo huo wakaonyesha ya kuwa hawako tayari kutoa hata siku moja kwa ajili ya kuzitakasa roho zao. Jambo hili likafanya Allah awakasirikie. Amri hii ya Sabato imetolewa katika Biblia (Kutoka 20:8-11); na kudhalilishwa kwao kwa sababu ya uasi huo kumetajwa katika Nehemia 13:15-18 na Jeremia 17:21-23.

Ama kusema ya kuwa Mayahudi waligeuka manyani hasa, ndivyo wasemavyo watu wasio na ujuzi wa kutosha. Kama mtu atasoma sura 5:61, 62 na sura 7:167-169, ataona wazi ya kuwa maelezo yaliyotolewa hapo kwa hao Mayahudi walioambiwa wawe manyani yanaonyesha kuwa, kwa umbo walikuwa ni watu hasa, tabia zao ndio zikawa za manyani na nguruwe.

Kadhalika katika nahau ya Kiarabu kama Mayahudi wale wangalikuwa wamegeuka wanyama hasa kwa umbo, wangesemwa *qiradatan khaasiatan.* Lakini kwa kuwa walikuwa ni watu ndio kusemwa *"qiradatan khaasi-iin"* kuonyesha kwamba walikuwa ni watu si wanyama.

Isitoshe wanazuoni wakubwa pia wamefahamu maneno hayo kwa maana hii hii tunayoieleza. Mathalan, Mujahid, ambaye ni mfasiri mkubwa sana wa Qur'an na aliyekuwa katika Matabii (yaani Waislamu walioonana na masahaba wa Mtume s.a.w.) ameeleza maneno hayo kwa maana hii hii tunayoieleza (Kathir).

فَجَعَلْنٰهَا نَكَالًا لِّمَا بَيْنَ يَدَيْهَا وَمَا خَلْفَهَا وَمَوْعِظَةً لِّلْمُتَّقِيْنَ ﴿٦٦﴾

67. Kwa hiyo Tukalifanya kuwa onyo kwa wale waliokuwa wakati huo na waliokuja nyuma yao, na mawaidha kwa wamchao Allah.

وَاِذْ قَالَ مُوْسٰى لِقَوْمِهٖٓ اِنَّ اللّٰهَ يَاْمُرُكُمْ اَنْ تَذْبَحُوْا بَقَرَةً ؕ قَالُوْٓا اَتَتَّخِذُنَا هُزُوًا ؕ قَالَ اَعُوْذُ بِاللّٰهِ اَنْ اَكُوْنَ مِنَ الْجٰهِلِيْنَ ﴿٦٧﴾

68. Na (kumbukeni) Musa alipowaambia watu wake: Hakika Allah anawaamuruni mchinje ng'ombe. Wakasema: Je, unatufanyia mzaha! Akasema: (La), najikinga kwa Allah nisiwe miongoni mwa wajinga.

قَالُوا ادْعُ لَنَا رَبَّكَ يُبَيِّنْ لَّنَا مَا هِيَ ؕ قَالَ اِنَّهٗ يَقُوْلُ اِنَّهَا بَقَرَةٌ لَّا فَارِضٌ وَّلَا بِكْرٌ ؕ عَوَانٌۢ بَيْنَ ذٰلِكَ ؕ فَافْعَلُوْا مَا تُؤْمَرُوْنَ ﴿٦٨﴾

69. Wakasema: Tuombee kwa Mola wako Atupambanulie ni yupi. Akasema: Hakika Yeye Anasema kwamba ng'ombe huyo si mzee wala si mchanga bali ni kijana baina ya hao. Basi fanyeni mnayoamrishwa.

قَالُوا ادْعُ لَنَا رَبَّكَ يُبَيِّنْ لَّنَا مَا لَوْنُهَا ؕ قَالَ اِنَّهٗ يَقُوْلُ اِنَّهَا بَقَرَةٌ صَفْرَآءُ ۙ فَاقِعٌ لَّوْنُهَا تَسُرُّ النّٰظِرِيْنَ ﴿٦٩﴾

70. Wakasema: Tuombee kwa Mola wako Atupambanulie rangi yake ikoje. Akasema: Hakika Yeye Anasema, hakika ng'ombe huyo ni wa manjano, rangi yake imeiva sana, huwapendeza watazamao.

قَالُوا ادْعُ لَنَا رَبَّكَ يُبَيِّنْ لَّنَا مَا هِيَ ۙ اِنَّ الْبَقَرَ تَشٰبَهَ عَلَيْنَا ؕ وَاِنَّآ اِنْ شَآءَ اللّٰهُ لَمُهْتَدُوْنَ ﴿٧٠﴾

71. Wakasema: Tuombee kwa Mola wako Atupambanulie ni yupi, hakika ng'ombe wote wanaonekana kwetu wamefanana; na kwa yakini kama Allah Akipenda tutakuwa wenye kuongoka.

Aya 67. *Onyo.* Adhabu inayotolewa kwa busara huwa itimize makusudio mawili; (1) kumtia maumivu mkosaji ili asirejee makosa baadaye; (2) adhabu hiyo iwe mawaidha kwa ajili ya watu wengine wajihadhari na kuangukia katika kosa la namna hiyo.

Aya 68. *Ng'ombe.* Waisraeli walikuwa wamekaa kwa miaka mingi pamoja na Wamisri ambao walikuwa wakimheshimu sana ng'ombe, na heshima ya ng'ombe ikapenya katika mioyo ya Waisraeli pia. Kuung'oa uovu huu walilazimishwa wawe wakichinja ng'ombe kwa sadaka maana watu hawawezi kumheshimu mnyama wanayemchinja.

قَالَ اِنَّهٗ يَقُوْلُ اِنَّهَا بَقَرَةٌ لَّا ذَلُوْلٌ تُثِيْرُ
الْاَرْضَ وَلَا تَسْقِى الْحَرْثَ ۚ مُسَلَّمَةٌ لَّا
شِيَةَ فِيْهَا ؕ قَالُوا الْـٰٔنَ جِئْتَ بِالْحَقِّ ؕ
فَذَبَحُوْهَا وَمَا كَادُوْا يَفْعَلُوْنَ ﴿٧١﴾ ع

72. Akasema: Hakika Yeye Anasema: Hakika huyo ni ng'ombe hakutiwa kazini kuilima ardhi wala kunyweshe-leza mimea, safi kabisa hana ila ndani yake. Wakasema: Sasa umeleta haki. Basi wakamchinja ijapokuwa (hapo kabla) wasingekuwa wenye kufanya hivyo.

FUNGU 9

وَاِذْ قَتَلْتُمْ نَفْسًا فَادّٰرَءْتُمْ فِيْهَا ؕ وَاللّٰهُ
مُخْرِجٌ مَّا كُنْتُمْ تَكْتُمُوْنَ ﴿٧٢﴾ ۚ

73. Na (kumbukeni) mlipoiua nafsi, kisha mkahitilafiana kwayo, na Allah ni mtoaji wa siri hiyo mliyokuwa mkiificha.

فَقُلْنَا اضْرِبُوْهُ بِبَعْضِهَا ؕ كَذٰلِكَ يُحْىِ اللّٰهُ
الْمَوْتٰى ۙ وَيُرِيْكُمْ اٰيٰتِهٖ لَعَلَّكُمْ
تَعْقِلُوْنَ ﴿٧٣﴾

74. Ndipo Tukasema: Lipigieni mfano (tukio) hilo kwa kulifananisha na matukio mengine kama hilo, ndivyo hivi Allah Huwahuisha wafu na Huwaonyesheni Ishara zake ili mpate kufahamu.

ثُمَّ قَسَتْ قُلُوْبُكُمْ مِّنْۢ بَعْدِ ذٰلِكَ فَهِىَ
كَالْحِجَارَةِ اَوْ اَشَدُّ قَسْوَةً ؕ وَاِنَّ مِنَ
الْحِجَارَةِ لَمَا يَتَفَجَّرُ مِنْهُ الْاَنْهٰرُ ؕ وَاِنَّ
مِنْهَا لَمَا يَشَّقَّقُ فَيَخْرُجُ مِنْهُ الْمَآءُ ؕ وَاِنَّ
مِنْهَا لَمَا يَهْبِطُ مِنْ خَشْيَةِ اللّٰهِ ؕ وَمَا اللّٰهُ
بِغَافِلٍ عَمَّا تَعْمَلُوْنَ ﴿٧٤﴾

75. Kisha baada ya hayo mioyo yenu ikawa migumu hata ikawa kama mawe au migumu zaidi; na hakika kuna mawe mengine yanayobubujika mito ndani yao, na hakika kuna mengine yanayopasukapasuka na yakatoa maji ndani yao; na hakika baadhi yao huanguka kwa sababu ya hofu ya Allah. Na Allah si mwenye kughafilika na mnayoyafanya.

اَفَتَطْمَعُوْنَ اَنْ يُّؤْمِنُوْا لَكُمْ وَقَدْ كَانَ
فَرِيْقٌ مِّنْهُمْ يَسْمَعُوْنَ كَلٰمَ اللّٰهِ ثُمَّ
يُحَرِّفُوْنَهٗ مِنْۢ بَعْدِ مَا عَقَلُوْهُ وَهُمْ
يَعْلَمُوْنَ ﴿٧٥﴾

76. Je, mnatumaini ya kwamba watakuaminini na hali kundi moja miongoni mwao lilikuwa linasikia maneno ya Allah, kisha (kwa makusudi) likawa linayabadili baada ya kuyafahamu na hali wanajua.

وَاِذَا لَقُوا الَّذِيْنَ اٰمَنُوْا قَالُوْٓا اٰمَنَّا ۚۖ
وَاِذَا خَلَا بَعْضُهُمْ اِلٰى بَعْضٍ قَالُوْٓا

77. Na wanapokutana na wale walioamini, husema Tumeamini, na wanapokuwa peke yao wao kwa wao,

husema: Je, mnawaambia (waaminio) Aliyowafungulieni Allah ili wapate kuhojiana nanyi mbele ya Mola wenu? Je, hamtumii akili?

اَتُحَدِّثُوْنَهُمْ بِمَا فَتَحَ اللّٰهُ عَلَيْكُمْ لِيُحَآجُّوْكُمْ بِهٖ عِنْدَ رَبِّكُمْ ؕ اَفَلَا تَعْقِلُوْنَ ﴿۷۷﴾

78. Je, hawajui ya kwamba Allah Anayajua wanayoyaficha na wanayoyadhihirisha?

اَوَلَا يَعْلَمُوْنَ اَنَّ اللّٰهَ يَعْلَمُ مَا يُسِرُّوْنَ وَمَا يُعْلِنُوْنَ ﴿۷۸﴾

79. Na wako miongoni mwao wasiojua kusoma: Hawajui Kitabu isipokuwa tamaa za upuuzi, nao hawana ila kudhania tu.

وَمِنْهُمْ اُمِّيُّوْنَ لَا يَعْلَمُوْنَ الْكِتٰبَ اِلَّاۤ اَمَانِيَّ وَاِنْ هُمْ اِلَّا يَظُنُّوْنَ ﴿۷۹﴾ ع

80. Basi ole kwa wale waandikao kitabu kwa mikono yao kisha husema hiki kimetoka kwa Allah ili wakiuze kwa thamani ndogo; basi ole wao kwa yale iliyoandika mikono yao na ole wao kwa yale wanayoyachuma.

فَوَيْلٌ لِّلَّذِيْنَ يَكْتُبُوْنَ الْكِتٰبَ بِاَيْدِيْهِمْ ۗ ثُمَّ يَقُوْلُوْنَ هٰذَا مِنْ عِنْدِ اللّٰهِ لِيَشْتَرُوْا بِهٖ ثَمَنًا قَلِيْلًا ؕ فَوَيْلٌ لَّهُمْ مِّمَّا كَتَبَتْ اَيْدِيْهِمْ وَوَيْلٌ لَّهُمْ مِّمَّا يَكْسِبُوْنَ ﴿۸۰﴾

81. Nao wanasema hautatugusa Moto kabisa isipokuwa kwa siku chache tu. Sema: Je, mmepata ahadi kwa Allah? Basi ndipo Allah Hataivunja ahadi Yake. Au mnasema juu ya Allah msiyoyajua?

وَقَالُوْا لَنْ تَمَسَّنَا النَّارُ اِلَّاۤ اَيَّامًا مَّعْدُوْدَةً ؕ قُلْ اَتَّخَذْتُمْ عِنْدَ اللّٰهِ عَهْدًا فَلَنْ يُّخْلِفَ اللّٰهُ عَهْدَهٗۤ اَمْ تَقُوْلُوْنَ عَلَى اللّٰهِ مَا لَا تَعْلَمُوْنَ ﴿۸۱﴾

82. Naam, anayechuma ubaya na makosa yake yakamzunguka, basi hao ndio watu wa motoni; humo watakaa muda mrefu.

بَلٰى مَنْ كَسَبَ سَيِّئَةً وَّاَحَاطَتْ بِهٖ خَطِيْٓـَٔتُهٗ فَاُولٰٓئِكَ اَصْحٰبُ النَّارِ ۚ هُمْ فِيْهَا خٰلِدُوْنَ ﴿۸۲﴾

83. Na wale walioamini na kutenda mema, hao ndio watu wa peponi, humo watakaa milele.

وَالَّذِيْنَ اٰمَنُوْا وَعَمِلُوا الصّٰلِحٰتِ اُولٰٓئِكَ اَصْحٰبُ الْجَنَّةِ ۚ هُمْ فِيْهَا خٰلِدُوْنَ ﴿۸۳﴾ ع ۹ ۱۱

Aya 80. *Wakiuze kwa thamani ndogo.* Mradi wake, si kama itafaa wakikiuza kwa thamani kubwa, bali ni kuwa thamani yo yote watakayopata itakuwa ni ndogo kwa kulinganisha na hasara watakayoipata kwa uovu wa namna hii.

FUNGU 10

وَاِذْ اَخَذْنَا مِيْثَاقَ بَنِيْٓ اِسْرَآءِيْلَ لَا
تَعْبُدُوْنَ اِلَّا اللّٰهَ ۖ وَبِالْوَالِدَيْنِ اِحْسَانًا
وَّذِى الْقُرْبٰى وَالْيَتٰمٰى وَالْمَسٰكِيْنِ
وَقُوْلُوْا لِلنَّاسِ حُسْنًا وَّاَقِيْمُوا الصَّلٰوةَ
وَاٰتُوا الزَّكٰوةَ ۭ ثُمَّ تَوَلَّيْتُمْ اِلَّا قَلِيْلًا
مِّنْكُمْ وَاَنْتُمْ مُّعْرِضُوْنَ ۝۸۳

84. Na (kumbukeni). Tulipofunga ahadi na wana wa Israeli: Hamtamwabudu ye yote ila Allah; na muwatendee kwa hisani wazazi na jamaa na mayatima na maskini; na semeni na watu kwa wema na simamisheni Sala na toeni Zaka; kisha mkakengeuka isipokuwa wachache tu miongoni mwenu nanyi mlikuwa mwendao upande.

وَاِذْ اَخَذْنَا مِيْثَاقَكُمْ لَا تَسْفِكُوْنَ
دِمَآءَكُمْ وَلَا تُخْرِجُوْنَ اَنْفُسَكُمْ مِّنْ
دِيَارِكُمْ ثُمَّ اَقْرَرْتُمْ وَاَنْتُمْ
تَشْهَدُوْنَ ۝۸۴

85. Na(kumbukeni)Tuliposhika ahadi yenu:hamtamwaga damu zenu,wala hamtawatoa watu wenu katika nyumba zenu; nanyi mkakubali na mnashuhudia.

ثُمَّ اَنْتُمْ هٰٓؤُلَآءِ تَقْتُلُوْنَ اَنْفُسَكُمْ
وَتُخْرِجُوْنَ فَرِيْقًا مِّنْكُمْ مِّنْ
دِيَارِهِمْ تَظٰهَرُوْنَ عَلَيْهِمْ بِالْاِثْمِ
وَالْعُدْوَانِ ۭ وَاِنْ يَّاْتُوْكُمْ اُسٰرٰى
تُفٰدُوْهُمْ وَهُوَ مُحَرَّمٌ عَلَيْكُمْ
اِخْرَاجُهُمْ ۭ اَفَتُؤْمِنُوْنَ بِبَعْضِ الْكِتٰبِ
وَتَكْفُرُوْنَ بِبَعْضٍ ۚ فَمَا جَزَآءُ مَنْ
يَّفْعَلُ ذٰلِكَ مِنْكُمْ اِلَّا خِزْيٌ فِي الْحَيٰوةِ
الدُّنْيَا ۚ وَيَوْمَ الْقِيٰمَةِ يُرَدُّوْنَ اِلٰٓى اَشَدِّ
الْعَذَابِ ۭ وَمَا اللّٰهُ بِغَافِلٍ عَمَّا تَعْمَلُوْنَ ۝۸۵

86. Kisha ninyi hao hao mnawaua watu wenu, na mnawatoa kundi moja miongoni mwenu kutoka kwenye maeneo yao, mkisaidiana dhidi yao kwa dhambi na uasi; na kama wakiwajieni mahabusu mnawakomboa, na hali imeharamishwa kwenu kuwatoa, Je, mnaamini baadhi ya Kitabu na kuyakataa mengine? Basi hakuna malipo kwa mwenye kufanya hayo katika ninyi ila fedheha katika maisha ya dunia, na siku ya Kiyama watarudishwa kwenye adhabu kali zaidi; na Allah si mwenye kughafilika na yale mnayoyatenda.

اُولٰۗىِٕكَ الَّذِيْنَ اشْتَرَوُا الْحَيٰوةَ
الدُّنْيَا بِالْاٰخِرَةِ ۠ فَلَا يُخَفَّفُ عَنْهُمُ
الْعَذَابُ وَلَا هُمْ يُنْصَرُوْنَ ۝۸۶ ع ۱۰

87. Hao ndio walionunua maisha ya dunia badala ya Akhera, kwa hiyo hawatapunguziwa adhabu wala hawatasaidiwa.

FUNGU 11

88. Na bila shaka Tulimpa Musa Kitabu na Tukafululiza kuwafuatisha Mitume (wengine) baada yake. Na Tukampa Isa mwana wa Mariamu Ishara zilizo wazi na Tukamsaidia kwa roho mtakatifu. Hivyo, je atakapokufikieni mtume yeyote na mambo msiyoyapenda ya aina hii mtafanya kiburi na kuwakadhibisha baadhi yao na kuwaua wengine?

وَلَقَدْ اٰتَيْنَا مُوْسَى الْكِتٰبَ وَقَفَّيْنَا مِنْۢ
بَعْدِهٖ بِالرُّسُلِ ۖ وَاٰتَيْنَا عِيْسَى ابْنَ مَرْيَمَ
الْبَيِّنٰتِ وَاَيَّدْنٰهُ بِرُوْحِ الْقُدُسِ ؕ اَفَكُلَّمَا
جَآءَكُمْ رَسُوْلٌۢ بِمَا لَا تَهْوٰٓى اَنْفُسُكُمُ
اسْتَكْبَرْتُمْ ۚ فَفَرِيْقًا كَذَّبْتُمْ ۗ وَفَرِيْقًا
تَقْتُلُوْنَ ﴿٨٨﴾

89. Na wakasema: Mioyo yetu imefunikwa. Bali Allah Amewalaani kwa kufuru zao, kwa hiyo ni kidogo tu wanayoyaamini.

وَقَالُوْا قُلُوْبُنَا غُلْفٌ ؕ بَلْ لَّعَنَهُمُ اللّٰهُ
بِكُفْرِهِمْ فَقَلِيْلًا مَّا يُؤْمِنُوْنَ ﴿٨٩﴾

90. Na kilipowafikia Kitabu kitokacho kwa Allah kisadikishacho yaliyo pamoja nao, na zamani walikuwa wakiomba ushindi juu ya makafiri; lakini yalipowafikia waliyoyatambua, wakayakataa; basi laana ya Allah iko juu ya makafiri.

وَلَمَّا جَآءَهُمْ كِتٰبٌ مِّنْ عِنْدِ اللّٰهِ
مُصَدِّقٌ لِّمَا مَعَهُمْ ۙ وَكَانُوْا مِنْ قَبْلُ
يَسْتَفْتِحُوْنَ عَلَى الَّذِيْنَ كَفَرُوْا ۚ فَلَمَّا
جَآءَهُمْ مَّا عَرَفُوْا كَفَرُوْا بِهٖ ۚ فَلَعْنَةُ
اللّٰهِ عَلَى الْكٰفِرِيْنَ ﴿٩٠﴾

Aya 88. *Ruuhul-Qudus.* "Maneno Matakatifu," Kadhalika maana yake ni Roho au Malaika Mtakatifu (Akrab na Lane). Tena *Ruuhul-Qudus* ni jina jingine la Malaika Jibrili (Jarir na Kathir). Nabii Isa kusaidiwa na *Ruuhul-Qudus* siyo maana yake Manabii wengine hawakusaidiwa naye, la; bali hapa ametajwa yeye kwa sababu Mayahudi ingawa walikiri jambo hili kwa Manabii wengine, hawakulikiri kwa Nabii Isa, na wakataka awaonyeshe ishara (Matt. 12:38-40) na pia wakamwona kama hana msaada wa Roho takatifu na kuwa alighilibiwa na pepo wachafu (Matt. 10:25 na Luka 11:15).

Hivyo Allah anataka kuwafahamisha Mayahudi kuwa kumkataa kwao Nabii Isa hakukuwa na haki.

Zisiyoyapenda nafsi zenu. Kila mara Manabii huleta mambo yasiyopendwa na watu ndiyo maana wanapofika, upinzani na uadui unatokea. Hii ndiyo mizani mojawapo ya kupimia ukweli wa Manabii. Kama Nabii ye yote akifika tumpime juu ya mizani hii, je, mambo anayoleta yanafurahiwa sana na watu au yanakasirikiwa?

Aya 89. *Imefunikwa,* yaani "imejaa elimu hatutaki mafundisho zaidi" au "sisi hatuwezi kufahamu."Hivyo ndivyo walivyokuwa wakijikurupusha Mayahudi wasitake kusikiliza haki.

Aya 90. *Yastaftihuuna,* "Wakiomba ushindi," pia ina maana hii, *wakidhihirisha*. Kwa maana hii ya pili, Mayahudi kabla ya Uislamu walikuwa wakidhihirisha kwa watu habari zilizomo katika Biblia za kufika Mtume. Lakini Mtume alipofika wakamkataa.

بِئْسَمَا اشْتَرَوْا بِهٖٓ اَنْفُسَهُمْ اَنْ يَّكْفُرُوْا بِمَآ اَنْزَلَ اللّٰهُ بَغْيًا اَنْ يُّنَزِّلَ اللّٰهُ مِنْ فَضْلِهٖ عَلٰى مَنْ يَّشَآءُ مِنْ عِبَادِهٖ ۚ فَبَآءُوْ بِغَضَبٍ عَلٰى غَضَبٍ ۭ وَلِلْكٰفِرِيْنَ عَذَابٌ مُّهِيْنٌ ﴿٩٠﴾

91. Ni kibaya walichouzia nafsi zao ya kuwa wanakataa Aliyoyateremsha Allah, kwa wivu, kwa sababu Allah Anateremsha fadhili Zake juu ya Amtakaye katika watumishi Wake. Kwa hiyo wakarudi na ghadhabu juu ya ghadhabu, na kwa makafiri iko adhabu ifedheheshayo.

وَاِذَا قِيْلَ لَهُمْ اٰمِنُوْا بِمَآ اَنْزَلَ اللّٰهُ قَالُوْا نُؤْمِنُ بِمَآ اُنْزِلَ عَلَيْنَا وَيَكْفُرُوْنَ بِمَا وَرَآءَهٗ ۤ وَهُوَ الْحَقُّ مُصَدِّقًا لِّمَا مَعَهُمْ ۭ قُلْ فَلِمَ تَقْتُلُوْنَ اَنْۢبِيَآءَ اللّٰهِ مِنْ قَبْلُ اِنْ كُنْتُمْ مُّؤْمِنِيْنَ ﴿٩١﴾

92. Na wanapoambiwa: Aminini Aliyoyateremsha Allah, husema: Tunaamini yaliyoteremshwa juu yetu; na huyakataa yaliyo minghairi ya hayo, nayo ndiyo haki inayosadikisha yale yaliyo pamoja nao. Sema: Basi kwa nini mlikuwa mkiwaua Mitume wa Allah hapo zamani kama ninyi ni waaminio?

وَلَقَدْ جَآءَكُمْ مُّوْسٰى بِالْبَيِّنٰتِ ثُمَّ اتَّخَذْتُمُ الْعِجْلَ مِنْۢ بَعْدِهٖ وَاَنْتُمْ ظٰلِمُوْنَ ﴿٩٢﴾

93. Na kwa hakika aliwafikieni Musa na Ishara waziwazi, kisha mkamshika ndama (kuwa mungu) baada yake, na mkawa wadhalimu.

وَاِذْ اَخَذْنَا مِيْثَاقَكُمْ وَرَفَعْنَا فَوْقَكُمُ الطُّوْرَ ۭ خُذُوْا مَآ اٰتَيْنٰكُمْ بِقُوَّةٍ وَّاسْمَعُوْا ۭ قَالُوْا سَمِعْنَا وَعَصَيْنَا ۤ وَاُشْرِبُوْا فِيْ قُلُوْبِهِمُ الْعِجْلَ بِكُفْرِهِمْ ۭ قُلْ بِئْسَمَا يَاْمُرُكُمْ بِهٖٓ اِيْمَانُكُمْ اِنْ كُنْتُمْ مُّؤْمِنِيْنَ ﴿٩٣﴾

94. Na (kumbukeni) Tuliposhika ahadi yenu na Tukainyanyua Tuur (mlima) juu yenu (Tukawaambieni): Shikeni kwa nguvuTuliyowapeni na sikilizeni. Wakasema: Tumesikia na tumekataa! Na wakanyweshwa mioyoni mwao (mapenzi ya) ndama kwa kufuru yao. Sema: Ni kibaya kinachowaamrisheni imani yenu ikiwa ninyi ni wenye kuamini.

قُلْ اِنْ كَانَتْ لَكُمُ الدَّارُ الْاٰخِرَةُ عِنْدَ اللّٰهِ خَالِصَةً مِّنْ دُوْنِ النَّاسِ فَتَمَنَّوُا الْمَوْتَ اِنْ كُنْتُمْ صٰدِقِيْنَ ﴿٩٤﴾

95. Sema: Ikiwa nyumba ya Akhera kwa Allah ni yenu tu bila ya watu wengine, basi tamanini mauti kama ninyi ni wakweli.

96. Nao hawatayatamani kabisa kwa sababu ya yale iliyoyatanguliza mikono yao; na Allah huwajua wadhalimu.

وَلَنْ يَّتَمَنَّوْهُ اَبَدًۢا بِمَا قَدَّمَتْ اَيْدِيْهِمْ ؕ
وَاللّٰهُ عَلِيْمٌۢ بِالظّٰلِمِيْنَ ﴿٩٦﴾

97. Na bila shaka utawaona wao ni wenye tamaa nyingi ya kuishi kuliko watu wengine, kiasi ya kwamba hata kuliko wale wamshirikishao Allah; kila mmoja wao anapenda laiti angepewa umri wa miaka elfu, na kupewa kwake umri mwingi kusingaliweza kumwondoa katika adhabu; na Allah Huyaona kwa kina wanayoyafanya.

وَلَتَجِدَنَّهُمْ اَحْرَصَ النَّاسِ عَلٰى حَيٰوةٍ ۚۛ
وَمِنَ الَّذِيْنَ اَشْرَكُوْا ۚۛ يَوَدُّ اَحَدُهُمْ لَوْ
يُعَمَّرُ اَلْفَ سَنَةٍ ۚ وَمَا هُوَ بِمُزَحْزِحِهٖ
مِنَ الْعَذَابِ اَنْ يُّعَمَّرَ ؕ وَاللّٰهُ بَصِيْرٌۢ بِمَا
يَعْمَلُوْنَ ﴿٩٧﴾ ع

معانقه ٢ عند المتاخرين

١١ ع ١٠ ١١

FUNGU 12

98. Sema: Yeyote aliye adui wa Jibrili (na aelewe); hakika yeye ndiye aliyeiteremsha moyoni mwako kwa idhini ya Allah, inayosadikisha yale yaliyokuwa kabla yake na ni mwongozo na habari njema kwa waaminio.

قُلْ مَنْ كَانَ عَدُوًّا لِّجِبْرِيْلَ فَاِنَّهٗ نَزَّلَهٗ
عَلٰى قَلْبِكَ بِاِذْنِ اللّٰهِ مُصَدِّقًا لِّمَا بَيْنَ
يَدَيْهِ وَهُدًى وَّبُشْرٰى لِلْمُؤْمِنِيْنَ ﴿٩٨﴾

99. Hivyo yeyote yule aliye adui wa Allah na Malaika wake na Mitume Wake na Jibrili na Mikaili, basi bila shaka Allah naye ni adui wa makafiri.

مَنْ كَانَ عَدُوًّا لِّلّٰهِ وَمَلٰٓئِكَتِهٖ وَرُسُلِهٖ
وَجِبْرِيْلَ وَمِيْكٰلَ فَاِنَّ اللّٰهَ عَدُوٌّ
لِّلْكٰفِرِيْنَ ﴿٩٩﴾

Aya 96. Katika Aya 95 Mayahudi wanaitwa waungane na Waislamu katika *Mubahala,* yaani mashindano ya kuomba dua. Wanaitwa kuomba pamoja na Waislamu ya kuwa Allah alete kifo au maangamizi kwa kundi ambalo Yeye Allah Analichukia na ambalo linashikilia njia ya uwongo.

Ikiwa ni kweli Mayahudi ndio vipenzi vya Allah, na Waislamu wamekasirikiwa naye, basi matokeo ya dua hiyo yatakuwa ni kuangamia kwa Waislamu, na hivyo itadhihirika ni kundi gani la haya mawili lililo upande wenye kweli.

Ushahidi ni mmoja tu unaoweza kuhakikisha ukweli wa madai yanayohitilafiana juu ya maisha ya Akhera ambayo huletwa na dini mbalimbali, nao ni huu ya kwamba, ahadi zinazotolewa kwa ajili ya maisha ya Akhera sehemu yake, japo ndogo, iweze kudhihirika katika dunia hii hii. Ikiwa katika mashindano ya kuomba dua kama hayo ya juu Allah angeonyesha upendo Wake kwa Mayahudi, ingehakikisha kabisa ya kuwa hata katika Akhera wao ndio watakaokuwa katika radhi ya Mwenyezi Mungu.

Qur'an imeendelea kusema ya kwamba Mayahudi hawatathubutu kupokea mashindano hayo maana wanajua sana yalivyo matendo yao na nia zao.

Habari zaidi za *Mubaahala* zimeelezwa katika sura 3:62.

وَلَقَدْ اَنْزَلْنَآ اِلَيْكَ اٰيٰتٍۢ بَيِّنٰتٍ ۚ وَمَا يَكْفُرُ بِهَآ اِلَّا الْفٰسِقُوْنَ ﴿٩٩﴾

100. Na kwa yakini Tulikuteremshia Ishara zilizo wazi, na hakuna wazikataao ila wavunjao amri.

اَوَكُلَّمَا عٰهَدُوْا عَهْدًا نَّبَذَهٗ فَرِيْقٌ مِّنْهُمْ ۭ بَلْ اَكْثَرُهُمْ لَا يُؤْمِنُوْنَ ﴿١٠٠﴾

101. Ala! Kila mara wanapofunga ahadi kundi moja katika wao wanaitupa? bali wengi wao hawaamini.

وَلَمَّا جَاۗءَهُمْ رَسُوْلٌ مِّنْ عِنْدِ اللّٰهِ مُصَدِّقٌ لِّمَا مَعَهُمْ نَبَذَ فَرِيْقٌ مِّنَ الَّذِيْنَ اُوْتُوا الْكِتٰبَ ۘ كِتٰبَ اللّٰهِ وَرَاۗءَ ظُهُوْرِهِمْ كَاَنَّهُمْ لَا يَعْلَمُوْنَ ﴿١٠١﴾

102. Na alipowafikia Mtume kutoka kwa Allah mwenye kusadikisha yale yaliyo pamoja nao, kundi moja miongoni mwa wale waliopewa Kitabu, likatupa kitabu cha Allah nyuma ya migongo yao kana kwamba hawajui.

وَاتَّبَعُوْا مَا تَتْلُوا الشَّيٰطِيْنُ عَلٰي مُلْكِ سُلَيْمٰنَ ۚ وَمَا كَفَرَ سُلَيْمٰنُ وَلٰكِنَّ الشَّيٰطِيْنَ كَفَرُوْا يُعَلِّمُوْنَ النَّاسَ السِّحْرَ ۗ وَمَآ اُنْزِلَ عَلَي الْمَلَكَيْنِ بِبَابِلَ هَارُوْتَ وَمَارُوْتَ ۭ وَمَا يُعَلِّمٰنِ مِنْ اَحَدٍ حَتّٰى يَقُوْلَآ اِنَّمَا نَحْنُ فِتْنَةٌ فَلَا تَكْفُرْ ۭ فَيَتَعَلَّمُوْنَ مِنْهُمَا مَا يُفَرِّقُوْنَ بِهٖ بَيْنَ الْمَرْءِ وَزَوْجِهٖ ۭ وَمَا هُمْ بِضَاۗرِّيْنَ بِهٖ مِنْ اَحَدٍ اِلَّا بِاِذْنِ اللّٰهِ ۭ وَيَتَعَلَّمُوْنَ مَا يَضُرُّهُمْ وَلَا يَنْفَعُهُمْ ۭ وَلَقَدْ عَلِمُوْا لَمَنِ اشْتَرٰىهُ مَا لَهٗ فِي الْاٰخِرَةِ مِنْ خَلَاقٍ ۣ وَلَبِئْسَ مَا شَرَوْا بِهٖٓ اَنْفُسَهُمْ ۭ لَوْ كَانُوْا يَعْلَمُوْنَ ﴿١٠٢﴾

103. Na wakayafuata yale waliyokuwa wakiyafuata mashetani dhidi ya ufalme wa Suleimani; na Suleimani hakukufuru, bali mashetani ndio waliokufuru, wakiwafundisha watu uchawi. Na (kinyume chake), yale yaliyoteremshwa huko Babil juu ya malaika wawili, Haruta na Maruta, (kisa chao ndio hiki kwamba) wao walikuwa hawamfundishi yeyote chochote mpaka wamuambie, hakika sisi ni jaribio basi usikatae. Hivyo watu wakajifunza kwao mambo yale yaliyokuwa yakileta mtengano kati ya mume na mke. Nao hawakuwa wenye kumdhuru ye yote kwa njia hiyo bila ya ruhusa ya Allah. Na (kinyume chake, kile walichokuwa wakijifunza watu wale kwa Mashetani), wao walikuwa wakijifunza mambo yale yaliyokuwa yakiwaletea hasara na kutowapatia faida, ilhali wao walikwisha fahamu vema kwamba yeyote aliyefanya biashara hiyo, huyo hatabakia na sehemu yoyote huko Akhera. Hivyo (faida hiyo ya muda mfupi) ambayo kwayo waliziuza nafsi zao ilikuwa ni mbaya mno, laiti wangalijua.

Aya 103. *Malakaini,* "Malaika wawili." Mradi wake ni *watu watawa wawili,* kama vile katika sura 12:32 Nabii Yusuf ameitwa *Malaika mtukufu* ilhali alikuwa mwanadamu.

Harut na *Marut* ni majina ya sifa. *Harut* maana yake *mchanaji. Marut* maana yake *mvunjaji* (Akrab). Majina haya yanaonyesha kazi za hao watawa wawili ilikuwa ni kuchana na kuvunja adhma na mamlaka ya watu fulani.

وَلَوْ اَنَّهُمْ اٰمَنُوْا وَاتَّقَوْا لَمَثُوْبَةٌ مِّنْ عِنْدِ اللّٰهِ خَيْرٌ ؕ لَوْ كَانُوْا يَعْلَمُوْنَ ﴿١٠٤﴾ ع ١٢

104. Na lau wangeamini na kuogopa bila shaka malipo yatokayo kwa Allah yangekuwa bora, laiti wangalijua!

FUNGU 13

يٰۤاَيُّهَا الَّذِيْنَ اٰمَنُوْا لَا تَقُوْلُوْا رَاعِنَا وَقُوْلُوا انْظُرْنَا وَاسْمَعُوْا ؕ وَلِلْكٰفِرِيْنَ عَذَابٌ اَلِيْمٌ ﴿١٠٥﴾

105. Enyi mlioamini, msiseme Raa'inaa bali semeni Undhurnaa na kusikiliza; na makafiri watapata adhabu iumizayo.

مَا يَوَدُّ الَّذِيْنَ كَفَرُوْا مِنْ اَهْلِ الْكِتٰبِ وَلَا الْمُشْرِكِيْنَ اَنْ يُّنَزَّلَ عَلَيْكُمْ مِّنْ خَيْرٍ مِّنْ رَّبِّكُمْ ؕ وَاللّٰهُ يَخْتَصُّ بِرَحْمَتِهٖ مَنْ يَّشَآءُ ؕ وَاللّٰهُ ذُو الْفَضْلِ الْعَظِيْمِ ﴿١٠٦﴾

106. Hawapendi waliokufuru miongoni mwa watu wa Kitabu wala washirikina mteremshiwe heri kutoka kwa Mola wenu, na Allah Humhusisha kwa rehema Zake Amtakaye; na Allah ndiye Mwenye fadhili kuu.

مَا نَنْسَخْ مِنْ اٰيَةٍ اَوْ نُنْسِهَا نَاْتِ بِخَيْرٍ مِّنْهَاۤ اَوْ مِثْلِهَا ؕ اَلَمْ تَعْلَمْ اَنَّ اللّٰهَ عَلٰى كُلِّ شَىْءٍ قَدِيْرٌ ﴿١٠٧﴾

107. Aya yo yote Tunayoifuta au kuisahaulisha Tunaleta iliyo bora kuliko ile au iliyo mfano wake; je, hujui kwamba Allah Anao uwezo juu ya kila kitu?

Ngano na visa vingi visivyokubaliwa na Qur'an wala hadithi za Mtume *s.a.w.* vinasimuliwa juu ya Aya hii. Haitafaa kabisa kufasiriwa Aya hii kwa kufuata visa hivyo, kama alivyosema Allama Abu Hayyan ya kuwa "haya yote si sahihi hata kidogo" (Muhit).

Aya 105. Msiseme *Raa'inaa,* maana neno hili lina maana mbili: (1) Tuangalie, (2) mpumbavu, mwenye majivuno na kiburi (Akrab). Neno hili walikuwa wanatumia Mayahudi kumwambia Mtume *s.a.w.* wakikusudia kumtukana kisirisiri. Basi waaminio bila kujua hila ya Mayahudi walianza kutumia neno hili, ndipo wakakatazwa na wakaambiwa watumie neno jingine *Undhurnaa* lenye maana moja tu, yaani, Utuangalie.

Aya 107. Katika Aya hii Allah ameeleza mambo mawili yanayofanyika, na matokeo mawili yanayopatana nayo. Mambo hayo ni *Kufuta* Aya na *Kusahaulisha*. Anapofuta, huleta *zilizo bora* kuliko zilizofutwa; na anaposahaulisha huleta *mfano wake.*

Mradi wa Aya zilizofutwa, ni sheria ya Musa na Vitabu vingine vya zamani, na badala yake Allah Akaleta Qur'an ambayo ni bora kuliko vitabu vya zamani. Na mradi katika kusahaulisha ni kama vile zamani baada ya kufika Taurati, kila iliposahauliwa Allah alileta Manabii wa kuyakumbusha na kuyaeleza vizuri mafundisho yake. Ama wale wanaokiri kuwa kuna Aya zingine za Qur'an zinazotangua zingine wanakosea kabisa. Kwanza fikira hiyo hata si sawa na akili kwamba maneno ya Allah yapinzane. Pili hakuna hata Hadithi moja ya Mtume s.a.w. inayokubali fikira hiyo, bali Mtume s.a.w. aliamrisha Qur'an yote ifuatwe

اَلَمْ تَعْلَمْ اَنَّ اللّٰهَ لَهٗ مُلْكُ السَّمٰوٰتِ وَالْاَرْضِ ؕ وَمَا لَكُمْ مِّنْ دُوْنِ اللّٰهِ مِنْ وَّلِيٍّ وَّلَا نَصِيْرٍ ﴿۱۰۸﴾

108. Je, hujui kwamba Allah ni Mwenye ufalme wa mbingu na ardhi? Nanyi hamna mlinzi mwingine wala msaidizi kinyume cha Allah.

اَمْ تُرِيْدُوْنَ اَنْ تَسْـَٔلُوْا رَسُوْلَكُمْ كَمَا سُئِلَ مُوْسٰى مِنْ قَبْلُ ؕ وَمَنْ يَّتَبَدَّلِ الْكُفْرَ بِالْاِيْمَانِ فَقَدْ ضَلَّ سَوَآءَ السَّبِيْلِ ﴿۱۰۹﴾

109. Je, mnataka kumwuliza Mtume wenu kama alivyoulizwa Musa zamani? Na anayebadilisha imani kwa kufuru, bila shaka ameipotea njia iliyo sawa.

وَدَّ كَثِيْرٌ مِّنْ اَهْلِ الْكِتٰبِ لَوْ يَرُدُّوْنَكُمْ مِّنْۢ بَعْدِ اِيْمَانِكُمْ كُفَّارًا ۚ حَسَدًا مِّنْ عِنْدِ اَنْفُسِهِمْ مِّنْۢ بَعْدِ مَا تَبَيَّنَ لَهُمُ الْحَقُّ ۚ فَاعْفُوْا وَاصْفَحُوْا حَتّٰى يَاْتِيَ اللّٰهُ بِاَمْرِهٖ ؕ اِنَّ اللّٰهَ عَلٰى كُلِّ شَيْءٍ قَدِيْرٌ ﴿۱۱۰﴾ ع

110. Wengi miongoni mwa watu wa Kitabu wanapenda wangewarudisheni ninyi muwe makafiri baada ya kuamini kwenu kwa sababu ya husuda iliyomo mioyoni mwao baada ya kuwapambanukia haki; basi sameheni na kuacha mpaka Allah Alete amri Yake; hakika Allah ni Mwenye uwezo juu ya kila kitu.

وَاَقِيْمُوا الصَّلٰوةَ وَاٰتُوا الزَّكٰوةَ ؕ وَمَا تُقَدِّمُوْا لِاَنْفُسِكُمْ مِّنْ خَيْرٍ تَجِدُوْهُ عِنْدَ اللّٰهِ ؕ اِنَّ اللّٰهَ بِمَا تَعْمَلُوْنَ بَصِيْرٌ ﴿۱۱۱﴾

111. Na simamisheni Sala na toeni Zaka; na heri mtakazozitanguliza kwa ajili ya nafsi zenu mtazikuta kwa Allah: hakika Allah Anayaona mnayoyafanya.

وَقَالُوْا لَنْ يَّدْخُلَ الْجَنَّةَ اِلَّا مَنْ كَانَ هُوْدًا اَوْ نَصٰرٰى ؕ تِلْكَ اَمَانِيُّهُمْ ؕ قُلْ هَاتُوْا بُرْهَانَكُمْ اِنْ كُنْتُمْ صٰدِقِيْنَ ﴿۱۱۲﴾

112. Nao husema: Hataingia Peponi ila aliye Myahudi au Mkristo! Hayo ndiyo matamanio yao. Sema: Leteni dalili yenu kama ninyi ni wakweli.

بَلٰى ۟ مَنْ اَسْلَمَ وَجْهَهٗ لِلّٰهِ وَهُوَ مُحْسِنٌ فَلَهٗۤ اَجْرُهٗ عِنْدَ رَبِّهٖ ۪ وَلَا خَوْفٌ عَلَيْهِمْ وَلَا هُمْ يَحْزَنُوْنَ ﴿۱۱۳﴾ ع ۱۳

113. Naam, ye yote anayejitupa kwa Allah, naye ni mtenda wema, basi yeye atapata malipo yake kwa Mola wake, wala haitakuwa hofu juu yao wala hawatahuzunika.

---

kabisa. Isitoshe Qur'an yenyewe inajishuhudia kuwa Aya zake zote zimehifadhiwa. (sura 15:10).

Maneno ya Qur'an hayapinzani hata kidogo. Anayeyaona yanapinzana ni kwa sababu haijui vizuri. Zaidi ya hayo wenye *naasikh* na *mansuukh* wamehitilafiana sana. Wengine wakisema zilizotanguka ni Aya mia kadha wa kadha. Na wengine wanakuja wakipunguza - punguza hesabu mpaka Aya tano. Lakini Seyyidna Ahmad a.s. aliyeijua vyema Qur'an, na ambaye ni Mujaddid wa zama hizi, ameeleza dalili nyingi kuhakikisha kuwa Aya za Qur'an hazitangui wala

FUNGU 14

وَقَالَتِ الْيَهُوْدُ لَيْسَتِ النَّصٰرٰى عَلٰى شَيْءٍ ۖ وَّقَالَتِ النَّصٰرٰى لَيْسَتِ الْيَهُوْدُ عَلٰى شَيْءٍ ۙ وَّهُمْ يَتْلُوْنَ الْكِتٰبَ ؕ كَذٰلِكَ قَالَ الَّذِيْنَ لَا يَعْلَمُوْنَ مِثْلَ قَوْلِهِمْ ۚ فَاللّٰهُ يَحْكُمُ بَيْنَهُمْ يَوْمَ الْقِيٰمَةِ فِيْمَا كَانُوْا فِيْهِ يَخْتَلِفُوْنَ ﴿١١٤﴾

114. Na Mayahudi husema: Wakristo hawakufungamana na cho chote; na Wakristo husema: Mayahudi hawakufungamana na cho chote; na hali wote wanasoma Kitabu; hivi ndivyo wasiojua walivyosema mfano wa kauli yao; basi Allah Atahukumu baina yao siku ya Kiyama katika yale waliyokuwa wakihitilafiana.

وَمَنْ اَظْلَمُ مِمَّنْ مَّنَعَ مَسٰجِدَ اللّٰهِ اَنْ يُّذْكَرَ فِيْهَا اسْمُهٗ وَسَعٰى فِيْ خَرَابِهَا ؕ اُولٰٓئِكَ مَا كَانَ لَهُمْ اَنْ يَّدْخُلُوْهَآ اِلَّا خَآئِفِيْنَ ؕ لَهُمْ فِي الدُّنْيَا خِزْيٌ وَّلَهُمْ فِي الْاٰخِرَةِ عَذَابٌ عَظِيْمٌ ﴿١١٥﴾

115. Na ni nani mdhalimu mkubwa kuliko yule azuiaye misikiti ya Allah ya kwamba humo lisitajwe jina Lake na kujitahidi kuiharibu? Haiwafai hao waingie ila kwa kuogopa. Hao watapata fedheha katika dunia na katika Akhera watapata adhabu kubwa.

---

hazitanguliwi kwani hazipinzani, bali kila neno la Qur'an litafanya kazi mpaka siku ya Kiyama.

Lakini Padre Dale kwa kutokujua hekima ya mpango wa maneno ya Qur'an, amesema kuwa Mtume *s.a.w.* "alisahau Aya nyingine," ilhali Allah amemwambia Mtume s.a.w., "Hivi karibuni tutakusomesha wala hutasahau" (sura 87:7). Pia tazama sura 75:17-20.

Aya 114. Sifa ya Qur'an ni kuwa inakubali mara moja uzuri wa kitu mahali ulipo. Hapa wanalaumiwa Mayahudi na Wakristo ambao ingawa wameshirikiana mambo mengi, na kitabu chao ni kile kile, lakini kila upande unakataa kabisa kuona mema yaliyoko upande mwingine. Lakini Qur'an iko tayari kukubali sifa ingawa ndogo iliyoko upande wo wote. Kama desturi ya namna hii ingeshikwa na watu wa dini nyingine, kukubalika mema yanayopatikana katika dini nyingine, suluhu kubwa ingeenea duniani.

Aya 115. Aya hii ni kemeo kali kwa watu wale wanaoshika uadui wa dini kwa kiasi hata hawajali kuharibu majumba ya ibada ya watu wa dini zingine, au wanawakataza watu wa dini zingine na madhehebu zingine kufanya ibada katika misikiti au nyumba zao za kuabudia.

Mtume *s.a.w.* aliwapa ruhusa Wakristo wa Najran, waliokuja Madina kushindana naye mambo ya dini, kufanya ibada katika Msikiti wake wa Madina (Zurkani). Kwa kushika kanuni hii ya Mtume *s.a.w.* Waahmadiyya walipojenga msikiti London, Hadhrat Amir-ul-Muminin, Khalifat-ul-Masih II, Seyyidna Mirza Bashir-ud-Din Mahmud Ahmad, (Mungu amrehemu), aliwatangazia watu wote katika mwaka 1924 huko Uingereza ruhusa ya kufanya ibada zao humo, haidhuru wawe dini gani. Kadhalika Jumuiya ya Ahmadiyya ilipojenga msikiti Tabora katika mwaka 1944, Sheikh Mubarak Ahmad, H.A. alitangaza ruhusa hii ya watu wa kila dini kuabudu humo, mbele ya Waafrika, Wahindi na Wazungu waliohudhuria katika sherehe ya kufunguliwa msikiti.

وَلِلّٰهِ الْمَشْرِقُ وَالْمَغْرِبُ ۚ فَاَيْنَمَا تُوَلُّوْا فَثَمَّ وَجْهُ اللّٰهِ ؕ اِنَّ اللّٰهَ وَاسِعٌ عَلِيْمٌ ﴿۱۱۵﴾

116. Na mashariki na magharibi ni ya Allah, basi mahali po pote mgeukiapo ndipo (mtaukuta) uso wa Allah. Bila shaka Allah ni Mwenye wasaa, Mwenye kujua.

وَقَالُوا اتَّخَذَ اللّٰهُ وَلَدًا سُبْحٰنَهٗ ؕ بَلْ لَّهٗ مَا فِي السَّمٰوٰتِ وَالْاَرْضِ ؕ كُلٌّ لَّهٗ قٰنِتُوْنَ ﴿۱۱۶﴾

117. Na wanasema, Allah amejipangia mwana. Ameepukana na hilo, bali ni Vyake vilivyomo mbinguni na ardhini. Vyote vinamtii Yeye.

بَدِيْعُ السَّمٰوٰتِ وَالْاَرْضِ ؕ وَاِذَا قَضٰۤى اَمْرًا فَاِنَّمَا يَقُوْلُ لَهٗ كُنْ فَيَكُوْنُ ﴿۱۱۷﴾

118. Mwanzishaji wa mbingu na ardhi; na Anapotaka jambo basi Huliambia tu, kuwa, nalo huwa.

وَقَالَ الَّذِيْنَ لَا يَعْلَمُوْنَ لَوْلَا يُكَلِّمُنَا اللّٰهُ اَوْ تَاْتِيْنَاۤ اٰيَةٌ ؕ كَذٰلِكَ قَالَ الَّذِيْنَ

119. Na wanasema wale wasiojua, mbona Allah Hasemi nasi au kutufikia Ishara? Hivyo walisema

---

Aya 116. *Na mashariki na magharibi ni ya Allah.* Katika Aya 115 Waarabu waliowazuilia Waislamu Msikiti Mtukufu waliahidiwa fedheha katika maisha ya dunia. Katika Aya hii Allah anawaahidi Waislamu kuwapa mashariki na magharibi, ijapokuwa katika siku zile walikuwa wamezungukwa na maadui pande zote. Katika miaka michache tu iliyofuata ahadi hii, Waislamu waliona msaada wa ajabu ukitoka kwa Mola wao, hata wakawa wafalme waliotawala sehemu kubwa za pande za mashariki.

Mtume *s.a.w.* alisema ya kwamba katika wakati wa Masih-ul-Mau'ud jua litakucha toka magharibi. Mradi wa hadithi hii ni kwamba Masihi atakapokuja, mafundisho yake yataenea upande wa magharibi pia, na watu wa huko watayashika na kuingia katika dini ya Kiislamu. Wabashiri wa Kiahmadiyya wamekwishafika nchi za Magharibi na watu wameanza kuukubali Uislamu.

Mwenye wasaa. Sifa hii inaonyesha ya kwamba hiyo ni ahadi ambayo inabidi kutimizwa wala isitiliwe shaka, maana Allah ni Mwenye wasaa,Aweza kuwapa watumishi Wake vyote vilivyomo duniani. Allah ni Mwenye elimu vile vile, Anajua bidii za watu na nia zao na vitendo vyao.

Aya hii, kama mnavyoona maelezo hayo, haielezi habari za Kibla au upande wa kuelekea wakati wa kusali, kama anavyodhania Padre Dale na kufikiri kuwa Aya hiyo imetanguka kwa vile Kibla inayoshikwa ni Makka. Bali Aya hiyo ni bishara kuwa Uislamu utaenea mashariki na magharibi. Katika siku za Mtume *s.a.w.* ulienea katika pande za mashariki. Na sasa katika siku za Masihi wake, Seyyidna Ahmad (amani juu yake), utaenea pande za magharibi, yaani Ulaya na Amerika; na ahadi hii kwa fadhili za Allah imekwisha anza kutimia pole pole.

Aya 117. *Mungu Amejipangia mwana.* Kuwa na mwana kunaonyesha upungufu na udhaifu. Allah ni Mtakatifu na Mkamilifu. Mwenye kudra na uwezo mtimilifu Alivyo Allah hawezi kuwa na mtoto. Aya inayofuata inaendelea kutia mkazo jambo hili.

مِنْ قَبْلِهِمْ مِّثْلَ قَوْلِهِمْ ؕ تَشَابَهَتْ قُلُوْبُهُمْ ؕ قَدْ بَيَّنَّا الْاٰيٰتِ لِقَوْمٍ يُّوْقِنُوْنَ ﴿۱۱۹﴾

wale waliokuwa kabla yao mfano wa kauli yao; mioyo yao imefanana. Hakika Sisi Tumezieleza Ishara kwa watu wenye yakini.

اِنَّاۤ اَرْسَلْنٰكَ بِالْحَقِّ بَشِيْرًا وَّ نَذِيْرًا ۙ وَّلَا تُسْـَٔلُ عَنْ اَصْحٰبِ الْجَحِيْمِ ﴿۱۱۹﴾

120. Hakika Sisi Tumekutuma na haki, kubashiri na kuonya, wala hutaulizwa habari za watu wa Motoni.

وَلَنْ تَرْضٰى عَنْكَ الْيَهُوْدُ وَلَا النَّصٰرٰى حَتّٰى تَتَّبِعَ مِلَّتَهُمْ ؕ قُلْ اِنَّ هُدَى اللّٰهِ هُوَ الْهُدٰى ؕ وَلَئِنِ اتَّبَعْتَ اَهْوَآءَهُمْ بَعْدَ الَّذِىْ جَآءَكَ مِنَ الْعِلْمِ ۙ مَا لَكَ مِنَ اللّٰهِ مِنْ وَّلِىٍّ وَّلَا نَصِيْرٍ ﴿۱۲۰﴾

121. Na hawatakuwa radhi juu yako Mayahudi wala Wakristo mpaka ufuate mila yao, Sema: Hakika mwongozo wa Allah ndio mwongozo hasa. Na kama ukifuata matamanio yao baada ya yale yaliyokufikia katika elimu, hutapata mlinzi wala msaidizi ye yote kwa Allah.

اَلَّذِيْنَ اٰتَيْنٰهُمُ الْكِتٰبَ يَتْلُوْنَهٗ حَقَّ تِلَاوَتِهٖ ؕ اُولٰٓئِكَ يُؤْمِنُوْنَ بِهٖ ؕ وَمَنْ يَّكْفُرْ بِهٖ فَاُولٰٓئِكَ هُمُ الْخٰسِرُوْنَ ﴿۱۲۱﴾

122. Wale Tuliowapa Kitabu wakakisoma kama ipasavyo kukisoma, hao ndio wanaokiamini; na anayekikataa basi hao ndio wenye hasara.

FUNGU 15

يٰبَنِىْۤ اِسْرَآءِيْلَ اذْكُرُوْا نِعْمَتِىَ الَّتِىْۤ اَنْعَمْتُ عَلَيْكُمْ وَاَنِّىْ فَضَّلْتُكُمْ عَلَى الْعٰلَمِيْنَ ﴿۱۲۲﴾

123. Enyi wana wa Israeli, kumbukeni neema Yangu Niliyowaneemesheni, nami Nikawafadhilini kuliko viumbe wengine.

وَاتَّقُوْا يَوْمًا لَّا تَجْزِىْ نَفْسٌ عَنْ نَّفْسٍ شَيْـًٔا وَّلَا يُقْبَلُ مِنْهَا عَدْلٌ وَّلَا تَنْفَعُهَا شَفَاعَةٌ وَّلَا هُمْ يُنْصَرُوْنَ ﴿۱۲۳﴾

124. Na iogopeni siku ambayo nafsi haitaifaa kitu nafsi nyingine, wala haitakubaliwa fidia kwake, wala maombezi hayataifaa, wala hawatasaidiwa.

وَاِذِ ابْتَلٰۤى اِبْرٰهٖمَ رَبُّهٗ بِكَلِمٰتٍ فَاَتَمَّهُنَّ ؕ قَالَ اِنِّىْ جَاعِلُكَ لِلنَّاسِ اِمَامًا ؕ قَالَ وَمِنْ ذُرِّيَّتِىْ ؕ قَالَ لَا يَنَالُ عَهْدِى الظّٰلِمِيْنَ ﴿۱۲۴﴾

125. Na (kumbukeni) Mola wake Alipompajaribu Ibrahimu kwa maneno, akayatimiza; Akasema: Hakika Mimi Nitakufanya Imamu wa watu. (Ibrahimu) akasema: Je, na katika wazao wangu pia? Akasema: (Ndiyo, lakini) ahadi Yangu haitawafikia wadhalimu.

Aya 125. *Kalimaatin*, "Maneno," yaani amri (Mufradat)

وَاِذْ جَعَلْنَا الْبَيْتَ مَثَابَةً لِّلنَّاسِ وَاَمْنًا ؕ وَاتَّخِذُوْا مِنْ مَّقَامِ اِبْرٰهٖمَ مُصَلًّى ؕ وَعَهِدْنَآ اِلٰٓى اِبْرٰهٖمَ وَاِسْمٰعِيْلَ اَنْ طَهِّرَا بَيْتِىَ لِلطَّآئِفِيْنَ وَالْعٰكِفِيْنَ وَالرُّكَّعِ السُّجُوْدِ ﴿١٢٥﴾

126. Na (kumbukeni) Tulipoifanya Nyumba iwe mahali pa kuendewa na watu na pa salama. Na mpafanye mahali aliposimama Ibrahimu pawe pa kusalia. Na Tuliwaagiza Ibrahimu na Ismaili kwamba ninyi wawili mwitakase Nyumba Yangu kwa ajili ya waizungukao na kwa wakaao na kwa wanaorukuu na kusujudu.

وَاِذْ قَالَ اِبْرٰهٖمُ رَبِّ اجْعَلْ هٰذَا بَلَدًا اٰمِنًا وَّارْزُقْ اَهْلَهٗ مِنَ الثَّمَرٰتِ مَنْ اٰمَنَ مِنْهُمْ بِاللّٰهِ وَالْيَوْمِ الْاٰخِرِ ؕ قَالَ وَمَنْ كَفَرَ فَاُمَتِّعُهٗ قَلِيْلًا ثُمَّ اَضْطَرُّهٗٓ اِلٰى عَذَابِ النَّارِ ؕ وَبِئْسَ الْمَصِيْرُ ﴿١٢٦﴾

127. Na (kumbukeni) aliposema Ibrahimu: Ee Mola wangu, Ufanye mji huu uwe wa salama na Uwape wenyeji wake matunda ,yule miongoni mwao anayemwamini Allah na siku ya Mwisho. (Allah) Akasema: Na mwenye kukufuru pia Nitamstarehesha kidogo kisha Nitamkokota kwenye adhabu ya Moto, napo ni mahali pabaya pa kurejea.

وَاِذْ يَرْفَعُ اِبْرٰهٖمُ الْقَوَاعِدَ مِنَ الْبَيْتِ وَاِسْمٰعِيْلُ ؕ رَبَّنَا تَقَبَّلْ مِنَّا ؕ اِنَّكَ اَنْتَ السَّمِيْعُ الْعَلِيْمُ ﴿١٢٧﴾

128. Na (kumbukeni) Ibrahimu alipoiinua misingi ya Nyumba, na Ismaili pia, (wakiomba): Ee Mola wetu, Utupokelee, hakika Wewe ndiwe Mwenye kusikia, Mwenye kujua.

Ahadi Yangu haitawafikia wadhalimu. Nabii Ibrahimu alipopewa unabii, aliomba wazao wake nao wapewe neema hiyo. Allah alikubali kuwa, ndiyo, unabii utaendelea, ila ahadi hiyo hawataipata wadhalimu.

Aya 126. *Mahali pa kuendewa na watu na pa salama.* Ahadi hii aliyopewa Ibrahimu na Allah imekwisha timia. Kaaba ni Nyumba inayoendewa na watu kila mwaka laki na laki wa mataifa mbalimbali na rangi mbalimbali, ambao wanaifikia kwa huba na shauku. Kadhalika Makka pamebakia peke yake mahali pa salama katika mahali pote patakatifu pa dini za dunia. Yerusalem na patakatifu pa dini zingine pamewahi kushambuliwa na maadui na kuangamizwa, lakini Makka siku zote imekaa katika mikono ya wanaoiheshimu.

Aya 127. Dua hii ilipoombwa na Nabii Ibrahimu, Makka ilikuwa ni jangwa tupu la ukiwa. Haikuwa na kitu ila Kaaba. Lakini sasa imekuwa mji mkubwa, maarufu, wenye matunda ya kila namna na watu na amani. Tazameni jinsi maombi haya ya Nabii Ibrahimu na mengine yanayotajwa katika Aya zijazo yalivyokubaliwa. Hii ni dalili ya kutosha kuonyesha kuwa yuko Allah anayesikia, Mwenye uwezo.

رَبَّنَا وَاجْعَلْنَا مُسْلِمَيْنِ لَكَ وَمِنْ ذُرِّيَّتِنَآ
أُمَّةً مُّسْلِمَةً لَّكَ ۠ وَأَرِنَا مَنَاسِكَنَا وَتُبْ
عَلَيْنَا ۚ إِنَّكَ أَنْتَ التَّوَّابُ الرَّحِيمُ ﴿١٢٩﴾

129. Ee Mola wetu, Utufanye tuwe wajitupao Kwako, na miongoni mwa wazao wetu pia Uwafanye watu wajitupao Kwako. Na Utuonyeshe njia za ibada yetu na Utuelekee; bila shaka Wewe ndiwe Mwelekevu, Mrehemevu.

رَبَّنَا وَابْعَثْ فِيهِمْ رَسُولًا مِّنْهُمْ يَتْلُوا
عَلَيْهِمْ آيَاتِكَ وَيُعَلِّمُهُمُ الْكِتَابَ
وَالْحِكْمَةَ وَيُزَكِّيهِمْ ۚ إِنَّكَ أَنْتَ
الْعَزِيزُ الْحَكِيمُ ﴿١٣٠﴾ ع

130. Ee Mola wetu, mwinue Mtume kati yao atokaye miongoni mwao, awasomee Aya Zako, na kuwafundisha Kitabu na hekima, na kuwatakasa. Hakika Wewe ndiwe Mwenye nguvu Mwenye hekima.

FUNGU 16

وَمَنْ يَرْغَبُ عَنْ مِّلَّةِ إِبْرَاهِيمَ إِلَّا مَنْ
سَفِهَ نَفْسَهُ ۚ وَلَقَدِ اصْطَفَيْنَاهُ فِي الدُّنْيَا ۖ
وَإِنَّهُ فِي الْآخِرَةِ لَمِنَ الصَّالِحِينَ ﴿١٣١﴾

131. Na nani atajitenga na mila ya Ibrahimu isipokuwa anayejipumbaza nafsi yake? Na kwa yakini Sisi Tulimchagua katika dunia, na kwa hakika yeye katika Akhera yu miongoni mwa watawa.

إِذْ قَالَ لَهُ رَبُّهُ أَسْلِمْ ۖ قَالَ أَسْلَمْتُ
لِرَبِّ الْعَالَمِينَ ﴿١٣٢﴾

132. (Kumbukeni) Mola wake Alipomwambia: Nyenyekea, akanena: Nanyenyekea kwa Mola wa walimwengu.

وَوَصَّىٰ بِهَا إِبْرَاهِيمُ بَنِيهِ وَيَعْقُوبُ ۚ
يَا بَنِيَّ إِنَّ اللَّهَ اصْطَفَىٰ لَكُمُ الدِّينَ
فَلَا تَمُوتُنَّ إِلَّا وَأَنْتُمْ مُّسْلِمُونَ ﴿١٣٣﴾

133. Na Ibrahimu akawausia hayo wanawe na Yakubu pia: Enyi wanangu, hakika Allah Amewachagulieni dini hii, basi msife ila nanyi mmekuwa wanyenyekeao.

Aya 130. *Mwinue Mtume.* Dua hii ya Nabii Ibrahimu, aliyoomba kwa moyo wake wote, ilitimia katika dhati ya Mtume Muhammad *s.a.w.* Namna Mtume alivyokuwa na sifa nne zilizoelezwa katika Aya hii ni jambo linalokubalika katika historia, ambalo hata maadui zake wajuvi kabisa wamelazimika kulikubali kuwa yeye ni Mtume aliyefanikiwa zaidi kuliko wengine wote. Mtume *s.a.w.* mwenyewe amesema , "Mimi ndiyo dua ya Ibrahimu" (Jarir na Asakir). Pia ikumbukwe ya kuwa Waarabu ni wazao wa Ismaili aliyekuwa mtoto wa Ibrahimu, na jambo hili ni hakika iliyokubaliwa na wanazuoni wa ulimwengu.

134. Je, mlikuwapo yalipomfikia Yakubu mauti, alipowaambia wanawe: Je, mtaabudu nini baada yangu? Wakasema: Tutamwabudu Mola wako na Mola wa baba zako, Ibrahimu na Ismaili na Isihaka, Mungu mmoja tu; na sisi tunanyenyekea Kwake.

اَمْ كُنْتُمْ شُهَدَآءَ اِذْ حَضَرَ يَعْقُوْبَ الْمَوْتُ ۙ اِذْ قَالَ لِبَنِيْهِ مَا تَعْبُدُوْنَ مِنْۢ بَعْدِيْ ؕ قَالُوْا نَعْبُدُ اِلٰهَكَ وَاِلٰهَ اٰبَآئِكَ اِبْرٰهٖمَ وَاِسْمٰعِيْلَ وَاِسْحٰقَ اِلٰهًا وَّاحِدًا ۚ وَّنَحْنُ لَهٗ مُسْلِمُوْنَ ﴿۱۳۳﴾

135. Hao ni watu waliokwisha pita, watapata waliyoyachuma nanyi mtapata mtakayoyachuma; wala hamtaulizwa yale waliyokuwa wakiyafanya.

تِلْكَ اُمَّةٌ قَدْ خَلَتْ ۚ لَهَا مَا كَسَبَتْ وَلَكُمْ مَّا كَسَبْتُمْ ۚ وَلَا تُسْـَٔلُوْنَ عَمَّا كَانُوْا يَعْمَلُوْنَ ﴿۱۳۴﴾

136. Na wakasema: Kuweni Mayahudi au Wakristo, mtaongoka. Sema: Bali (shikeni) mila ya Ibrahimu aliyehalisika, wala hakuwa miongoni mwa washirikina.

وَقَالُوْا كُوْنُوْا هُوْدًا اَوْ نَصٰرٰى تَهْتَدُوْا ؕ قُلْ بَلْ مِلَّةَ اِبْرٰهٖمَ حَنِيْفًا ؕ وَمَا كَانَ مِنَ الْمُشْرِكِيْنَ ﴿۱۳۵﴾

137. Semeni: Tumemwamini Allah na yale tuliyoteremshiwa na yaliyoteremshwa kwa Ibrahimu na Ismaili na Isihaka na Yakubu na wazao (wake), na pia yale aliyopewa Musa na Isa na yale waliyopewa Manabii kutoka kwa Mola wao; hatutofautishi baina ya mmoja kati yao; na sisi tumejitupa Kwake.

قُوْلُوْٓا اٰمَنَّا بِاللّٰهِ وَمَآ اُنْزِلَ اِلَيْنَا وَمَآ اُنْزِلَ اِلٰٓى اِبْرٰهٖمَ وَاِسْمٰعِيْلَ وَاِسْحٰقَ وَيَعْقُوْبَ وَالْاَسْبَاطِ وَمَآ اُوْتِيَ مُوْسٰى وَعِيْسٰى وَمَآ اُوْتِيَ النَّبِيُّوْنَ مِنْ رَّبِّهِمْ ۚ لَا نُفَرِّقُ بَيْنَ اَحَدٍ مِّنْهُمْ ۖ وَنَحْنُ لَهٗ مُسْلِمُوْنَ ﴿۱۳۶﴾

138. Basi wakiamini kama mnavyomwamini ninyi, kweli wameongoka; na wakikengeuka, basi bila shaka wao wamo katika upinzani tu. Basi bila shaka Allah Atakutosheleza kwao; na Yeye ndiye Asikiaye, Ajuaye.

فَاِنْ اٰمَنُوْا بِمِثْلِ مَآ اٰمَنْتُمْ بِهٖ فَقَدِ اهْتَدَوْا ۚ وَاِنْ تَوَلَّوْا فَاِنَّمَا هُمْ فِيْ شِقَاقٍ ۚ فَسَيَكْفِيْكَهُمُ اللّٰهُ ۚ وَهُوَ السَّمِيْعُ الْعَلِيْمُ ﴿۱۳۷﴾

139. (jipakeni) Rangi ya Allah; na ni nani aliye mbora wa rangi kuliko Allah? Na ni Yeye tu ndiye tunamwabudu.

صِبْغَةَ اللّٰهِ ۚ وَمَنْ اَحْسَنُ مِنَ اللّٰهِ صِبْغَةً ۖ وَّنَحْنُ لَهٗ عٰبِدُوْنَ ﴿۱۳۸﴾

Aya 139. *Sibgha*, "rangi," mradi wake ni (1) dini; (2) kanuni za sheria; (3) tabia ambayo

قُلْ اَتُحَآجُّوْنَنَا فِى اللّٰهِ وَهُوَ رَبُّنَا وَرَبُّكُمْ ۚ وَلَنَآ اَعْمَالُنَا وَلَكُمْ اَعْمَالُكُمْ ۚ وَنَحْنُ لَهٗ مُخْلِصُوْنَ ﴿١٣٩﴾

140. Sema: Je, mnahojiana nasi juu ya Allah na hali Yeye ni Mola wetu na Mola wenu? Na vitendo vyetu ni kwa ajili yetu na vitendo vyenu ni kwa ajili yenu; nasi tunajihalisisha Kwake.

اَمْ تَقُوْلُوْنَ اِنَّ اِبْرٰهٖمَ وَاِسْمٰعِيْلَ وَاِسْحٰقَ وَيَعْقُوْبَ وَالْاَسْبَاطَ كَانُوْا هُوْدًا اَوْ نَصٰرٰى ؕ قُلْ ءَاَنْتُمْ اَعْلَمُ اَمِ اللّٰهُ ؕ وَمَنْ اَظْلَمُ مِمَّنْ كَتَمَ شَهَادَةً عِنْدَهٗ مِنَ اللّٰهِ ؕ وَمَا اللّٰهُ بِغَافِلٍ عَمَّا تَعْمَلُوْنَ ﴿١٤٠﴾

141. Je, mnasema: Hakika Ibrahimu na Ismaili na Isihaka na Yakubu na wazao (wake) walikuwa Mayahudi au Wakristo? Sema: Je, ninyi mnajua zaidi au Allah? Na ni nani mdhalimu mkubwa kuliko yule afichaye ushahidi alio nao utokao kwa Allah? Na Allah si Mwenye kughafilika na hayo mnayoyafanya.

تِلْكَ اُمَّةٌ قَدْ خَلَتْ ۚ لَهَا مَا كَسَبَتْ وَلَكُمْ مَّا كَسَبْتُمْ ۚ وَلَا تُسْـَٔلُوْنَ عَمَّا كَانُوْا يَعْمَلُوْنَ ﴿١٤١﴾ ع ١٢

142. Hao ndio watu waliokwisha pita, watapata waliyoyachuma, na ninyi mtapata mtakayoyachuma; wala hamtaulizwa yale waliyokuwa wakiyafanya.

JUZU 2.

FUNGU 17

سَيَقُوْلُ السُّفَهَآءُ مِنَ النَّاسِ مَا وَلّٰىهُمْ

143. Karibuni wapumbavu miongoni mwa watu watasema: Nini kimewageuza ١٣ ع

Allah amempa mtu; (4) ubatizo (Akrab). Dini inaitwa sibgha kwa sababu inamwenea mtu kama rangi. Hivyo *sibghatallahi* maana yake ni "shika au fuata dini ambayo Allah anakutaka uishike au uifuate." Huo ndio hasa ubatizo wa kweli unaoweza kumfanya mtu aige sifa za Allah. Ubatizo huu ni Mtukufu na mbali kabisa na ubatizo wa Kikristo ambao unatafuta kumpatia mtu kusamehewa dhambi zake, na kumpatia mtu uhai wa milele, kwa tendo dogo la kumchovya ndani ya maji au kumnyunyuziayo wakati wa kumtia Ukristo.

Dini ya Allah haina maana kwamba Allah anafuata dini yo yote ile. Ina maana tu kwamba ni ile dini iliyofunuliwa na Allah.

Aya 142. Mayahudi na Wakristo wanakumbushwa mara ya tena ya kuwa wasitegemee babu zao waliomridhisha Allah kwa vitendo vyao vyema. Vitendo vyao tu, siyo vya watu wengine, ndivyo vinavyoweza kuwaokoa. Wakitenda mema wataokoka wala siyo kwa sababu wao ni watoto wa Ibrahimu, au Yakubu, au wa Musa na Isa.

Aya 143. *Nini kimewageuza*. Ilikuwa desturi ya Mtume s.a.w. kuafikiana na watu wa

katika Kibla chao walichokuwa wakielekea? Sema: Mashariki na Magharibi ni ya Allah; Humwongoza Amtakaye kwenye njia iliyonyooka.

عَنْ قِبْلَتِهِمُ الَّتِيْ كَانُوْا عَلَيْهَا ؕ قُلْ لِّلّٰهِ
الْمَشْرِقُ وَالْمَغْرِبُ ؕ يَهْدِيْ مَنْ يَّشَآءُ اِلٰى
صِرَاطٍ مُّسْتَقِيْمٍ ﴿١٤٣﴾

144. Na vivyo Tumewafanyeni umati wa wastani ili muwe mashahidi juu ya watu, na Mtume awe shahidi juu yenu. Na Hatukukifanya Kibla ulichokuwa nacho ila Tupate kujulisha yule anayemfuata Mtume kutoka yule anayegeuka kwa visigino vyake; na kwa yakini ilikuwa jambo gumu isipokuwa kwa wale Aliowaongoza Allah; Na Allah si Mwenye kuzipoteza imani zenu, bila shaka Allah kwa watu ni Mpole sana Mrehemevu.

وَكَذٰلِكَ جَعَلْنٰكُمْ اُمَّةً وَّسَطًا لِّتَكُوْنُوْا
شُهَدَآءَ عَلَى النَّاسِ وَيَكُوْنَ الرَّسُوْلُ
عَلَيْكُمْ شَهِيْدًا ؕ وَمَا جَعَلْنَا الْقِبْلَةَ الَّتِيْ
كُنْتَ عَلَيْهَآ اِلَّا لِنَعْلَمَ مَنْ يَّتَّبِعُ
الرَّسُوْلَ مِمَّنْ يَّنْقَلِبُ عَلٰى عَقِبَيْهِ ؕ وَاِنْ
كَانَتْ لَكَبِيْرَةً اِلَّا عَلَى الَّذِيْنَ هَدَى اللّٰهُ ؕ
وَمَا كَانَ اللّٰهُ لِيُضِيْعَ اِيْمَانَكُمْ ؕ اِنَّ اللّٰهَ
بِالنَّاسِ لَرَءُوْفٌ رَّحِيْمٌ ﴿١٤٤﴾

Kitabu katika mambo ambayo alikuwa hajafunuliwa na Allah. Imeandikwa katika Bukhari, "Mtume *s.a.w.* alikuwa akiwafikiana na watu wa Kitabu katika mambo asiyoyaamrishwa" (Bukhari, jalada 2 uk. 169). Basi Mtume *s.a.w.* alipokuwa katika mji wa Makka kwa miaka 13 alikuwa akielekea *Bait-ul-Mukaddas* wakati wa kusali, ingawa moyo wake ulikuwa ukipenda kuelekea Kibla ya Nabii Ibrahimu, yaani Kaaba, lakini asitake kufanya hivyo pasipo amri ya Allah. Katika Makka ilikuwa rahisi kuzielekea Kibla zote mbili, Kaaba na *Bait-ul-Mukaddas.* Lakini alipohamia Madina ilikuwa haiwezekani kuzielekea Kibla zote mbili. Mtume s.a.w. asitake kuelekea Kaaba mpaka apate amri ya Allah. Hivyo akaendelea kuelekea *Bait-ul-Mukaddas* kwa miezi 16 baada ya kuhamia Madina, mpaka alipoambiwa na Allah kuelekea Kaaba, basi akaielekea.

Basi katika Aya hii na zingine zifuatazo Allah anawajibu wakinzani na anathibitisha usafihi wao. Jambo la ajabu ni hili ya kuwa maneno haya: "Karibuni wapumbavu miongoni mwa watu watasema" yanatimiza ukweli unaoendelea kila siku, kwani watu wameendelea kupinza jambo hili pasipo na akili. Kwa mfano upinzani mmoja ulioelezwa ni kusema, "Labda Mtume *s.a.w.* alitaka kuvuta mioyo ya Mayahudi na Wakristo, na alipoona kuwa hawapatikani, alitoa amri waigeukie Kaaba." Lakini mtu mwenye akili anaweza kufahamu kuwa upinzani huu si haki, sababu yake ni hii kwamba katika Makka kulikuwa na Waarabu wengi wasioamini. Ingekuwa ni kutaka kuwapendeza watu, Mtume *s.a.w.* angeelekea Kaaba ambayo ni Nyumba waliyokuwa wakiiheshimu sana. Lakini Mtume *s.a.w.* alielekea Kibla cha Mayahudi. Na katika Madina ambako Mayahudi na Wakristo walikuwa wengi, Mtume *s.a.w.* akaelekea upande wa Kaaba. Je, kwa njia ya namna hii mtu anaweza kuwafurahisha watu? Basi upinzani wa namna hii unathibitisha tu ukweli wa maneno ya Allah, "Karibuni wapumbavu watasema. ....."

Aya 144. *Tupate kujulisha yule anayemfuata Mtume.* Kwa kugeuza Kibla washirikina wa Bara Arabu na watu wa Kitabu (Mayahudi na Wakristo) wote walijaribiwa kuwa ni nani anayesikiliza sauti ya mbingu na ni nani anayefuata matamanio ya nafsi yake. Kwanza kwa kuelekea

قَدْ نَرٰى تَقَلُّبَ وَجْهِكَ فِي السَّمَآءِ ۚ
فَلَنُوَلِّيَنَّكَ قِبْلَةً تَرْضٰىهَا ۪ فَوَلِّ وَجْهَكَ
شَطْرَ الْمَسْجِدِ الْحَرَامِ ؕ وَحَيْثُ مَا كُنْتُمْ
فَوَلُّوْا وُجُوْهَكُمْ شَطْرَهٗ ؕ وَاِنَّ الَّذِيْنَ
اُوْتُوا الْكِتٰبَ لَيَعْلَمُوْنَ اَنَّهُ الْحَقُّ مِنْ
رَّبِّهِمْ ؕ وَمَا اللّٰهُ بِغَافِلٍ عَمَّا يَعْمَلُوْنَ ﴿۱۴۵﴾

145. Kwa yakini Tumeona uso wako ukielekea mbinguni, basi bila shaka Tutakugeuza kwenye Kibla ukipendacho, na geuza uso wako upande wa Msikiti Mtakatifu, na po pote mnapokuwa zielekezeni nyuso zenu uliko; na hakika wale waliopewa Kitabu wanajua sana kwamba hiyo ni haki itokayo kwa Mola wao; na Allah si Mwenye kughafilika na yale wanayoyatenda.

وَلَئِنْ اَتَيْتَ الَّذِيْنَ اُوْتُوا الْكِتٰبَ بِكُلِّ
اٰيَةٍ مَّا تَبِعُوْا قِبْلَتَكَ ۚ وَمَآ اَنْتَ بِتَابِعٍ
قِبْلَتَهُمْ ۚ وَمَا بَعْضُهُمْ بِتَابِعٍ قِبْلَةَ بَعْضٍ ؕ
وَلَئِنِ اتَّبَعْتَ اَهْوَآءَهُمْ مِّنْۢ بَعْدِ مَا
جَآءَكَ مِنَ الْعِلْمِ ۙ اِنَّكَ اِذًا لَّمِنَ
الظّٰلِمِيْنَ ﴿۱۴۶﴾

146. Na hata ukiwaletea waliopewa Kitabu Ishara za kila namna hawatafuata Kibla chako; wala wewe hutafuata Kibla chao; wala baadhi yao hawafuati Kibla cha wengine wao; na kama ukiyafuata matamanio yao baada ya kukufikia elimu, hakika hapo utakuwa miongoni mwa wadhalimu.

اَلَّذِيْنَ اٰتَيْنٰهُمُ الْكِتٰبَ يَعْرِفُوْنَهٗ كَمَا
يَعْرِفُوْنَ اَبْنَآءَهُمْ ؕ وَاِنَّ فَرِيْقًا مِّنْهُمْ
لَيَكْتُمُوْنَ الْحَقَّ وَهُمْ يَعْلَمُوْنَ ﴿۱۴۷﴾

147. Wale Tuliowapa Kitabu wanamtambua (Mtume s.a.w. baada ya kuona athari za kimbingu ndani mwake) kama wanavyowatambua wana wao; lakini baadhi yao wanaficha ukweli kwa makusudi hali wanajua.

Bait-ul-Mukaddas walijaribiwa Waarabu, maana wao wasingependa asilan kuelekea Kibla cha Mayahudi. Na kwa kugeuza Kibla ikawa jaribio kwa ajili ya Mayahudi na Wakristo. Basi jambo hilo likamtofautisha mwema na mbaya.

Allah hakuwa mwenye kuipoteza imani yenu. Kwa kugeuza Kibla haiwezi kuharibika imani ya Waislamu, bali itakuwa imara zaidi, maana sasa itathibitika kuwa wale wanaostahili baraka za Ibrahimu ni wale wale wanaofuata Kibla kilichoamrishwa.

Aya 145. *Po pote mnapokuwa zielekezeni nyuso zenu uliko.* Amri hii si kwa ajili ya Waislamu wa Madina tu, bali ni kwa ajili ya waislamu wote wa ulimwengu, ili kuthibitisha umoja katika mambo yao yote.

Aya 147. *"Wamemtambua (Mtume s.a.w. baada ya kuona athari za kimbingu ndani mwake) kama wanavyowatambua wana wao".* Mradi wake ni zile ishara za ukweli ambazo wanazishuhudia katika mwenendo wa Mtukufu Mtume s.a.w. Ni dhahiri kwamba yu mtu mcha-Mungu kwa sababu anabainisha sifa za Allah. Kama vile wawatambuavyo watoto wao kutokana na alama na chapa za tabia zao wenyewe zilizojitokeza kwa watoto hao hivyo basi kuwajua kwamba ni watoto wao kwelikweli, vivyo hivyo mtu wa Mungu ni lazima atambulike kutokana na sifa za Allah ambazo zinaonyeshwa katika mwenendo wake na njia ya maisha yake.

148. Ndiyo haki iliyotoka kwa Mola wako, basi usiwe miongoni mwa wafanyao shaka.

اَلْحَقُّ مِنْ رَّبِّكَ فَلَا تَكُوْنَنَّ مِنَ الْمُمْتَرِيْنَ ﴿١٤٨﴾ ع ١٧

FUNGU 18

149. Na kila mtu anayo shabaha anayoielekea; basi shindaneni katika mema; po pote mtakapokuwa Allah Atawaleteni nyote pamoja; kwa yakini Allah ni mweza wa kila kitu.

وَلِكُلٍّ وِّجْهَةٌ هُوَ مُوَلِّيْهَا فَاسْتَبِقُوا الْخَيْرٰتِ ؕ اَيْنَ مَا تَكُوْنُوْا يَاْتِ بِكُمُ اللّٰهُ جَمِيْعًا ؕ اِنَّ اللّٰهَ عَلٰى كُلِّ شَىْءٍ قَدِيْرٌ ﴿١٤٩﴾

150. Na po pote utokapo geuza uso wako kwenye Msikiti Mtakatifu, na bila shaka hiyo ndiyo haki itokayo kwa Mola wako, na Allah si Mwenye kughafilika na yale mnayoyatenda.

وَمِنْ حَيْثُ خَرَجْتَ فَوَلِّ وَجْهَكَ شَطْرَ الْمَسْجِدِ الْحَرَامِ ؕ وَاِنَّهٗ لَلْحَقُّ مِنْ رَّبِّكَ ؕ وَمَا اللّٰهُ بِغَافِلٍ عَمَّا تَعْمَلُوْنَ ﴿١٥٠﴾

151. Na po pote utokapo geuza uso wako kwenye Msikiti Mtakatifu, na po pote mlipo geuzeni nyuso zenu uliko, ili watu wasiwe na hoja juu yenu, isipokuwa waliodhulumu miongoni mwao, basi msiwaogope, bali Niogopeni Mimi, ili Nitimize neema zangu juu yenu na ili mpate kuongoka.

وَمِنْ حَيْثُ خَرَجْتَ فَوَلِّ وَجْهَكَ شَطْرَ الْمَسْجِدِ الْحَرَامِ ؕ وَحَيْثُ مَا كُنْتُمْ فَوَلُّوْا وُجُوْهَكُمْ شَطْرَهٗ ۙ لِئَلَّا يَكُوْنَ لِلنَّاسِ عَلَيْكُمْ حُجَّةٌ ۗ اِلَّا الَّذِيْنَ ظَلَمُوْا مِنْهُمْ فَلَا تَخْشَوْهُمْ وَاخْشَوْنِىْ ۗ وَلِاُتِمَّ نِعْمَتِىْ عَلَيْكُمْ وَلَعَلَّكُمْ تَهْتَدُوْنَ ﴿١٥١﴾

Aya 148. *Ndiyo haki iliyotoka kwa Mola wako,* ewe msomaji wa hii Qur'an, usiwe na shaka juu ya mambo yanayoelezwa katika Kitabu hiki Kitukufu, maana ukweli wa mambo haya huthibitika.

Aya 149. *Shindaneni katika mema*. Kila mtu analo kusudi maalumu, na analiangalia sana katika vitendo vyake vyote. Basi kusudi la Waislamu linatakiwa liwe kushindana katika mema, yaani kila mmoja wao afanye bidii kuwapita wenzake katika mema.

Aya 150. *Na po pote utokapo.* Mtume Muhammad *s.a.w.* anaambiwa ya kuwa maadam sasa mmeamrishwa kuelekea Kaaba, imekuwa lazima kwako kufanya bidii kuupata mji wa Makka, ili Kaaba iwe mikononi mwa Waislamu

Aya 151. *Ili watu wasiwe na hoja juu yenu.* Ilikuwa lazima Mtume *s.a.w.* ashinde Makka, ili wasio Waislamu wasipate nafasi ya kusema, "Waislamu wanahubiri umoja wa Allah, lakini mbona Kibla chao kimejaa masanamu!"

كَمَآ اَرْسَلْنَا فِيْكُمْ رَسُوْلًا مِّنْكُمْ يَتْلُوْا عَلَيْكُمْ اٰيٰتِنَا وَيُزَكِّيْكُمْ وَيُعَلِّمُكُمُ الْكِتٰبَ وَالْحِكْمَةَ وَيُعَلِّمُكُمْ مَّا لَمْ تَكُوْنُوْا تَعْلَمُوْنَ ﴿١٥١﴾

152. Kama Tulivyomtuma Mtume kwenu kutoka miongoni mwenu, anawasomeeni Aya Zetu na kuwatakaseni na kuwafundisheni Kitabu na hekima na kuwafundisheni mliyokuwa hamyajui.

فَاذْكُرُوْنِيْٓ اَذْكُرْكُمْ وَاشْكُرُوْا لِيْ وَلَا تَكْفُرُوْنِ ﴿١٥٢﴾ ع ١٨ ٢

153. Basi mnikumbuke, (nami) Nitawakumbukeni; na Nishukuruni wala msinikufuru.

FUNGU 19

يٰٓاَيُّهَا الَّذِيْنَ اٰمَنُوا اسْتَعِيْنُوْا بِالصَّبْرِ وَالصَّلٰوةِ ؕ اِنَّ اللّٰهَ مَعَ الصّٰبِرِيْنَ ﴿١٥٣﴾

154. Enyi mlioamini, ombeni msaada kwa subira na Sala; bila shaka Allah Yu pamoja na wanaosubiri.

وَلَا تَقُوْلُوْا لِمَنْ يُّقْتَلُ فِيْ سَبِيْلِ اللّٰهِ اَمْوَاتٌ ؕ بَلْ اَحْيَآءٌ وَّ لٰكِنْ لَّا تَشْعُرُوْنَ ﴿١٥٤﴾

155. Wala msiwaite wale waliouwawa katika njia ya Allah kuwa wafu, bali ni wazima lakini ninyi hamtambui.

وَلَنَبْلُوَنَّكُمْ بِشَيْءٍ مِّنَ الْخَوْفِ وَالْجُوْعِ وَنَقْصٍ مِّنَ الْاَمْوَالِ وَالْاَنْفُسِ وَالثَّمَرٰتِ ؕ وَبَشِّرِ الصّٰبِرِيْنَ ﴿١٥٥﴾

156. Na kwa yakini Tutawajaribuni kwa jambo la hofu na kwa njaa na kwa upungufu wa mali na watu na matunda; na uwapashe habari njema wanaosubiri,

---

Aya 153. *Mnikumbuke, (nami) Nitawakumbukeni*. Binadamu kumkumbuka Allah ni kumpenda, kuzifuata amri Zake, na kumtukuza. Na Allah kumkumbuka binadamu ni kumhurumia, kumneemesha na kumwongoza katika njia Zake.

Aya 154. Waaminio wameahidiwa kupata msaada wa Allah kwa kushika njia mbili: (1) *Subira* - waaminio wajizoeze kuvumilia na wasiache desturi ya dini katika taabu na mashaka; (2) *Sala* - wadumu kusali. Hivyo Allah atakuwa pamoja nao.

Aya 155. Kifo ni kitu cha lazima kwa kila mtu. Allah amekwisha sema, *kullu nafsin dhaaiqatul maut* (Kila nafsi itaonja mauti sura 3:186). Lakini katika Aya hii Allah anasema ya kuwa tusiwaite kuwa ni wafu wale waliouwawa katika njia yake. Mradi wa uzima huu ni namna tatu: (1) Kazi yao itaendelea na haitakufa, na hivyo watakumbukwa daima; (2) Hawakufa bure: watu wengi atapata uzima wa kiroho kwa ajili ya juhudi yao; (3) Roho zao zitafufuliwa upesi katika maisha mapya.

Aya 156. *Tutawajaribuni.* Wema wa mtu na ubaya wake hujulikana wakati wa mitihani. Na yule ambaye anataka kupata cheo kikubwa ni lazima apite katika majaribio. Basi Allah anawaambia Waislamu kwamba, kupata neema Zangu na baraka Zangu mtapata, lakini ni sharti mkashinde katika majaribio niliyoyaweka.

الَّذِيْنَ اِذَآ اَصَابَتْهُمْ مُّصِيْبَةٌ ۙ قَالُوْٓا
اِنَّا لِلّٰهِ وَ اِنَّآ اِلَيْهِ رٰجِعُوْنَ ﴿١٥٧﴾

157. Ambao uwapatapo msiba husema: Hakika sisi ni wa Allah, na bila shaka Kwake tutarejea.

اُولٰٓئِكَ عَلَيْهِمْ صَلَوٰتٌ مِّنْ رَّبِّهِمْ
وَ رَحْمَةٌ ۟ وَ اُولٰٓئِكَ هُمُ الْمُهْتَدُوْنَ ﴿١٥٨﴾

158. Hao juu yao ziko baraka na rehema kutoka kwa Mola wao, nao ndio wenye kuongoka.

اِنَّ الصَّفَا وَ الْمَرْوَةَ مِنْ شَعَآئِرِ اللّٰهِ ۚ فَمَنْ
حَجَّ الْبَيْتَ اَوِ اعْتَمَرَ فَلَا جُنَاحَ عَلَيْهِ اَنْ
يَّطَّوَّفَ بِهِمَا ؕ وَ مَنْ تَطَوَّعَ خَيْرًا ۙ فَاِنَّ
اللّٰهَ شَاكِرٌ عَلِيْمٌ ﴿١٥٩﴾

159. Hakika Safaa na Marwa ni katika alama za Allah; basi anayehiji kwenye Nyumba au kufanya Umra si kosa kwake kuvizunguka (vilima) hivyo viwili; na anayefanya wema kwa shauku ya nafsi yake, basi Allah ni Mwenye shukurani Ajuaye.

اِنَّ الَّذِيْنَ يَكْتُمُوْنَ مَآ اَنْزَلْنَا مِنَ الْبَيِّنٰتِ
وَ الْهُدٰى مِنْۢ بَعْدِ مَا بَيَّنّٰهُ لِلنَّاسِ فِى
الْكِتٰبِ ۙ اُولٰٓئِكَ يَلْعَنُهُمُ اللّٰهُ وَ يَلْعَنُهُمُ
اللّٰعِنُوْنَ ﴿١٦٠﴾ۙ

160. Hakika wale wanaoficha Tuliyoyateremsha katika Ishara zilizo wazi na mwongozo, baada ya sisi kuzibainisha kwa watu Kitabuni, Hao ndio Atakaowalaani Allah na walaanio (wengine pia) watawalaani.

اِلَّا الَّذِيْنَ تَابُوْا وَ اَصْلَحُوْا وَ بَيَّنُوْا فَاُولٰٓئِكَ
اَتُوْبُ عَلَيْهِمْ ۚ وَ اَنَا التَّوَّابُ الرَّحِيْمُ ﴿١٦٠﴾

161. Ila wale waliotubu na kujisahihisha na kubainisha, basi hao Nitawaelekea, na Mimi ni Mwelekevu sana, Mwenye rehema.

Aya 157. *Sisi ni wa Allah,* yaani wanakuwa radhi juu ya radhi ya Allah, hawaonyeshi chuki wakati wa misiba wala hawafi moyo.

Aya 159. *Safaa na Marwa* ni vilima viwili vya Makka vilivyoko karibu na Kaaba. Nabii Ibrahimu alimwacha mkewe, Hajira, na mwanawe, Ismaili, karibu na vilima hivyo kwa amri ya Allah. Ismaili alikuwa bado mtoto mchanga. Kiu ya maji ilimshika na akakaribia kufa. Mama yake asiweze kuvumilia kuona mwanawe akifa katika hali ya namna hii, basi akaanza kutafuta maji. Akapanda na kuteremka juu ya vilima hivyo mara saba katika kutafuta maji, mpaka Malaika wa Mungu akamwambia, "Ewe Hajira, nenda utakuta chemchem ya maji karibu na mtoto wako." Hajira akarudi na akakuta maji yakitoka zam zam zam. Na kwa ajili hii chemchem ile inaitwa mpaka leo Zam Zam. (Bukhari).

Vilima hivyo vinakumbusha subira na sadaka ya Hajira na Ismaili. Sasa watu wanaokwenda kuhiji wanafanya kama alivyofanya Hajira alipokuwa anatafuta maji, ili wapate kujua kuwa anayekubali taabu kwa ajili ya Allah, hubarikiwa na kupata fadhili Zake.

Si kosa kwake. Kabla ya dini ya Kiislamu, Waarabu waliweka masanamu mawili juu ya Safaa na Marwa. Kwa ajili hii Waislamu wakafikiri labda ni vibaya kuvizunguka vilima hivyo. Basi, wanaambiwa si kosa kuvizunguka.

اِنَّ الَّذِيْنَ كَفَرُوْا وَمَاتُوْا وَهُمْ كُفَّارٌ
اُولٰٓئِكَ عَلَيْهِمْ لَعْنَةُ اللّٰهِ وَالْمَلٰٓئِكَةِ
وَالنَّاسِ اَجْمَعِيْنَ ﴿١٦٢﴾

162. Hakika waliokufuru na wakafa hali ni makafiri, hao ndio iko juu yao laana ya Allah, na ya Malaika na ya watu wote.

خٰلِدِيْنَ فِيْهَا ۚ لَا يُخَفَّفُ عَنْهُمُ الْعَذَابُ
وَلَا هُمْ يُنْظَرُوْنَ ﴿١٦٣﴾

163. Humo watakaa. Hawatapunguziwa adhabu, wala hawatapumzishwa.

وَاِلٰهُكُمْ اِلٰهٌ وَّاحِدٌ ۚ لَآ اِلٰهَ اِلَّا هُوَ
الرَّحْمٰنُ الرَّحِيْمُ ﴿١٦٤﴾ ع ١٥

164. Na Mungu wenu ni Mungu Mmoja, hakuna aabudiwaye ila Yeye, Mwingi wa rehema Mwingi wa ukarimu.

FUNGU 20

اِنَّ فِيْ خَلْقِ السَّمٰوٰتِ وَالْاَرْضِ
وَاخْتِلَافِ الَّيْلِ وَالنَّهَارِ وَالْفُلْكِ الَّتِيْ
تَجْرِيْ فِي الْبَحْرِ بِمَا يَنْفَعُ النَّاسَ وَمَآ
اَنْزَلَ اللّٰهُ مِنَ السَّمَآءِ مِنْ مَّآءٍ فَاَحْيَا بِهِ
الْاَرْضَ بَعْدَ مَوْتِهَا وَبَثَّ فِيْهَا مِنْ كُلِّ
دَآبَّةٍ ۖ وَّ تَصْرِيْفِ الرِّيٰحِ وَالسَّحَابِ
الْمُسَخَّرِ بَيْنَ السَّمَآءِ وَالْاَرْضِ لَاٰيٰتٍ
لِّقَوْمٍ يَّعْقِلُوْنَ ﴿١٦٥﴾

165. Hakika katika kuumbwa kwa mbingu na ardhi, na mfuatano wa usiku na mchana, na vyombo ambavyo hupita katika bahari kwa (kuchukua vitu) viwafaavyo watu, na maji Aliyoyateremsha Allah kutoka mawinguni, na kwayo Akaihuisha ardhi baada ya kufa kwake, na humo Akaeneza kila aina ya wanyama; na mabadiliko ya pepo, na mawingu yaliyotiishwa kati ya mbingu na ardhi, bila shaka zimo Ishara kwa watu wenye kutumia akili.

وَمِنَ النَّاسِ مَنْ يَّتَّخِذُ مِنْ دُوْنِ اللّٰهِ
اَنْدَادًا يُّحِبُّوْنَهُمْ كَحُبِّ اللّٰهِ ؕ وَالَّذِيْنَ
اٰمَنُوْٓا اَشَدُّ حُبًّا لِّلّٰهِ ؕ وَلَوْ يَرَى الَّذِيْنَ
ظَلَمُوْٓا اِذْ يَرَوْنَ الْعَذَابَ ۙ اَنَّ الْقُوَّةَ لِلّٰهِ
جَمِيْعًا ۙ وَّاَنَّ اللّٰهَ شَدِيْدُ الْعَذَابِ ﴿١٦٦﴾

166. Na katika watu wako wanaoshika washirika kinyume cha Allah, wanawapenda kama kumpenda Allah. Wakati wale walioamini wanampenda Allah zaidi (kuliko vitu vyote) ; na laiti waliodhulumu wangalijua watakapoiona adhabu, ya kwamba nguvu zote ni za Allah, na kwamba Allah ni mkali wa kuadhibu.

Aya 165. Waaminio wanahimizwa kupeleleza na kuchungua habari za ulimwengu.

167. Wale waliofuatwa watakapowachukia wale waliofuata na kuiona adhabu ilhali njia zote za wokovu zitakuwa zimekatika.

اِذْ تَبَرَّاَ الَّذِيْنَ اتُّبِعُوْا مِنَ الَّذِيْنَ اتَّبَعُوْا وَرَاَوُا الْعَذَابَ وَتَقَطَّعَتْ بِهِمُ الْاَسْبَابُ ﴿١٦٧﴾

168. Na watasema wale waliofuata, Laiti tungeweza kurudi (duniani), tungaliwakataa kama wanavyotukataa. Hivi ndivyo Allah Atakavyowaonyesha vitendo vyao kuwa majuto juu yao, wala hawatakuwa wenye kutoka Motoni.

وَقَالَ الَّذِيْنَ اتَّبَعُوْا لَوْ اَنَّ لَنَا كَرَّةً فَنَتَبَرَّاَ مِنْهُمْ كَمَا تَبَرَّءُوْا مِنَّا ؕ كَذٰلِكَ يُرِيْهِمُ اللّٰهُ اَعْمَالَهُمْ حَسَرٰتٍ عَلَيْهِمْ ؕ وَمَا هُمْ بِخٰرِجِيْنَ مِنَ النَّارِ ﴿١٦٨﴾ ع ٢

FUNGU 21

169. Enyi watu! kuleni katika vile vilivyomo ardhini, vilivyo halali na vyenye kufaa kiafya, wala msifuate nyayo za Shetani; bila shaka yeye kwenu ni adui dhahiri.

يٰۤاَيُّهَا النَّاسُ كُلُوْا مِمَّا فِى الْاَرْضِ حَلٰلًا طَيِّبًا ۖ وَّلَا تَتَّبِعُوْا خُطُوٰتِ الشَّيْطٰنِ ؕ اِنَّهٗ لَكُمْ عَدُوٌّ مُّبِيْنٌ ﴿١٦٩﴾

170. Yeye huwaamuruni tu mambo mabaya na ya aibu, na kuwa mseme juu ya Allah msiyoyajua.

اِنَّمَا يَاْمُرُكُمْ بِالسُّوْٓءِ وَالْفَحْشَآءِ وَاَنْ تَقُوْلُوْا عَلَى اللّٰهِ مَا لَا تَعْلَمُوْنَ ﴿١٧٠﴾

Aya 169. *Vilivyo halali na vyenye kufaa kiafya*. Ni wazi kuwa chakula huleta athari juu ya kiwiliwili cha mtu na juu ya roho yake pia. Chakula kisicho halali huharibu imani ya mtu, maana ni kunyume cha amri ya Mwumbaji wake. Na chakula ambacho si kizuri hudhuru kiwiliwili chake. Basi, ilikuwa lazima kwa dini iliyo kamili kueleza habari kamili katika jambo hili. Islam inasema: (1) Chakula kiwe halali, yaani kilichoruhusiwa na sheria ya Allah. (2) Kiwe kizuri kinachofaa kiwiliwili cha binadamu. Maana mwenye kiwiliwili kibaya na roho najisi hawezi kutimiza kusudi la kuumbwa kwake.

Neno *twayyib* linaweza kutumika katika uchaguzi wa mtu binafsi na pia hali ya uzuri kiafya wa kile kitu ambacho kimetangazwa kuwa halali. Katika maana ya kwanza chakula kile kile ambacho ni halali chaweza kuwa *twayyib* kwa mtu mmoja na kikawa siyo *twayyib* kwa watu wengine kutokana na kuhitilafiana katika uchaguzi, muonjo na mazingira. Katika maana ya pili neno *twayyib* laweza kuirejea ile hali ya chakula likiashiria kwamba waaminio wanapendelea kula chakula ambacho siyo tu ni halali bali pia chapatikana katika hali nzuri, ya uzima na ya kiafya.

Wakristo hawana kanuni yo yote juu ya vyakula na hakuna chakula cho chote kilicho najisi kwao (1 Wakor, 10:25-27; Tito 1:15) Ati wanasema pombe si haramu maana inaingia ndani (Marko 7:15-19). Lakini kutukana ni haramu sababu matusi yanatoka nje. Lakini hawatambui kuwa pombe ikiingia ndani mtu hupata kichaa, na anaweza kumtukana hata baba yake, aliyemzaa. Basi kitu kibaya kilipoingia ndani kimetoa kitu kibaya. Hivyo kama pombe ingeharimishwa, machafu mengi yangezuilika.

171. Na wanapoambiwa: Fuateni Aliyoyateremsha Allah, husema: Bali, tutafuata yale tuliyowakuta nayo baba zetu. Je, hata kama baba zao walikuwa hawafahamu cho chote wala hawakuongoka?

وَاِذَا قِيْلَ لَهُمُ اتَّبِعُوْا مَآ اَنْزَلَ اللّٰهُ قَالُوْا بَلْ نَتَّبِعُ مَآ اَلْفَيْنَا عَلَيْهِ اٰبَآءَنَا ؕ اَوَلَوْ كَانَ اٰبَآؤُهُمْ لَا يَعْقِلُوْنَ شَيْـًٔا وَّلَا يَهْتَدُوْنَ ﴿۱۷۰﴾

172. Na mfano wa wale waliokufuru ni kama mfano wa yule anayemwita asiyesikia ila sauti na kelele tu; ni viziwi, mabubu, vipofu, kwa hiyo hawafahamu.

وَمَثَلُ الَّذِيْنَ كَفَرُوْا كَمَثَلِ الَّذِيْ يَنْعِقُ بِمَا لَا يَسْمَعُ اِلَّا دُعَآءً وَّنِدَآءً ؕ صُمٌّۢ بُكْمٌ عُمْيٌ فَهُمْ لَا يَعْقِلُوْنَ ﴿۱۷۱﴾

173. Enyi mlioamini, kuleni katika vitu vizuri Tulivyowaruzukuni, na Mshukuruni Allah, ikiwa mnamwabudu Yeye tu.

يٰۤاَيُّهَا الَّذِيْنَ اٰمَنُوْا كُلُوْا مِنْ طَيِّبٰتِ مَا رَزَقْنٰكُمْ وَاشْكُرُوْا لِلّٰهِ اِنْ كُنْتُمْ اِيَّاهُ تَعْبُدُوْنَ ﴿۱۷۲﴾

174. Yeye Amewaharamishieni tu mzoga na damu na nyama ya nguruwe, na kilichosomewa ghairi ya jina la Allah; lakini aliyeshurutishwa, bila kutamani wala kupita kiasi, basi yeye hana dhambi; hakika Allah ni Msamehevu, Mrehemevu.

اِنَّمَا حَرَّمَ عَلَيْكُمُ الْمَيْتَةَ وَالدَّمَ وَلَحْمَ الْخِنْزِيْرِ وَمَآ اُهِلَّ بِهٖ لِغَيْرِ اللّٰهِ ۚ فَمَنِ اضْطُرَّ غَيْرَ بَاغٍ وَّلَا عَادٍ فَلَاۤ اِثْمَ عَلَيْهِ ؕ اِنَّ اللّٰهَ غَفُوْرٌ رَّحِيْمٌ ﴿۱۷۳﴾

Aya 171. *Tuliyowakuta nayo baba zetu.* Ni jambo la kushangaza kuwa watu wanawafuata wazee wao katika khabari za dini kama vile vipofu pasipo kupeleleza. Allah hataki hivyo, bali Anataka kila mtu aamini baada ya kupeleleza mwenyewe, si kwa kuwafuata wazee. Lakini hao hao wanaowafuata wazee wao mara moja katika habari za dini, hawafuati nyayo zao katika ustaarabu wa kidunia, ila wanafuata mambo yanayoonekana mazuri kwao.

Aya 172. Mfano wa Mtume *s.a.w.* na makafiri ni kama mchungaji na wanyama; ambaye huwaita wanyama wake wasiofahamu kusudi la maneno anenayo.

Aya 174. *Mzoga na damu na nyama ya nguruwe.* Amri za sheria zinamwezesha mfuasi wake kuishi maisha ya usafi, uzima na mafanikio. Sheria inaeleza mambo mengi ya manufaa ambayo tusingeweza kuyagundua kwa akili yetu peke yake ila baada ya usumbufu mwingi na juhudi ya miaka mingi. Kwa hakika kufuata sheria za Allah kunamwinua mtu hali yake na kuongoza akili yake na mawazo yake.

Qur'an inahimiza kutenda matendo mazuri. Na njia moja ya kutenda hayo ni kutumia vyakula vizuri na vifaavyo. Katika sura 2:169 kutumia vitu halali na vifaavyo kumeamrishwa, na sura 23:52 inaeleza mafungamano yaliyoko baina ya vyakula visafi na matendo mema.

175. Kwa yakini wale wafichao Aliyoyateremsha Allah katika Kitabu na kukiuza kwa bei ndogo, hao hawali matumboni mwao isipokuwa moto, wala Allah hatazungumza nao siku ya Kiyama, wala Hatawatakasa; nao watapata adhabu iumizayo.

إِنَّ الَّذِيْنَ يَكْتُمُوْنَ مَآ اَنْزَلَ اللّٰهُ مِنَ الْكِتٰبِ وَيَشْتَرُوْنَ بِهٖ ثَمَنًا قَلِيْلًا ۙ اُولٰٓئِكَ مَا يَاْكُلُوْنَ فِيْ بُطُوْنِهِمْ اِلَّا النَّارَ وَلَا يُكَلِّمُهُمُ اللّٰهُ يَوْمَ الْقِيٰمَةِ وَلَا يُزَكِّيْهِمْ ۚ وَلَهُمْ عَذَابٌ اَلِيْمٌ ﴿١٧٥﴾

176. Hao ndio walionunua upotevu kwa uongofu, na adhabu kwa ghofira; je, wana ujasiri gani wa kuvumilia Moto!

اُولٰٓئِكَ الَّذِيْنَ اشْتَرَوُا الضَّلٰلَةَ بِالْهُدٰى وَالْعَذَابَ بِالْمَغْفِرَةِ ۚ فَمَآ اَصْبَرَهُمْ عَلَى النَّارِ ﴿١٧٦﴾

177. Hayo ni kwa sababu Allah Ameteremsha Kitabu kwa haki; na hakika wale waliohitilafiana katika Kitabu kwa yakini wamo katika upinzani wa mbali.

ذٰلِكَ بِاَنَّ اللّٰهَ نَزَّلَ الْكِتٰبَ بِالْحَقِّ ؕ وَاِنَّ الَّذِيْنَ اخْتَلَفُوْا فِي الْكِتٰبِ لَفِيْ شِقَاقٍ بَعِيْدٍ ﴿١٧٧﴾ ع ٢١

BIBILIA JUU YA VYAKULA

Vitu vilivyoharimishwa katika sheria ya Kiislamu havikuruhusiwa katika Biblia. Mzoga, damu na nyama ya nguruwe vimekatazwa katika Biblia (Walawi 11). Mayahudi walishikilia tu maagizo ya vyakula na amri zingine za nje wakasahau kusudi kubwa la sheria - kumpenda Allah na kutenda mema, hata wakakataa Mitume wa Allah waliowaletea usafi wa moyo na tabia njema. Wakristo walitafuta kumridhisha Allah bila ya kufuata sheria Yake, wakapotea. Paulo anasema, "Kila kitu kiuzwacho sokoni kuleni, bila kuuliza-uliza, kwa ajili ya dhamiri; maana dunia ni mali ya Bwana na vyote viijazavyo. Na mtu asiyeamini akiwaalika, nanyi mnataka kwenda , kuleni kila kitu kiwekwacho mbele yenu, bila kuuliza-uliza" (1 Wakor. 10:25-27). Tena anasema, "Vitu vyote ni safi kwa hao walio safi; lakini hakuna kilicho safi kwao walio wanajisi, wasioamini" (Tito 1:15). Akaandika tena, Kila kiumbe cha Mungu ni kizuri, wala hakuna cha kukataliwa, kama kikipokewa kwa shukurani" (1 Timotheo 4:4, 5)

Ni dhahiri ya kwamba maneno hayo ambayo wanayashikilia sana Wakristo ni kinyume cha Qur'an na sheria ya Musa. Hatuna ujuzi zaidi kumshinda Allah. Yeye akisema kitu fulani ni najisi tutakataaje? Tena hatuwezi kupokea kilicho najisi kwa shukurani, wala shukurani hiyo haitakubaliwa; maana shukurani ya namna ile ni kumchezea Mungu na sheria Yake.

Mzoga umekatazwa na sababu zake ni hizi:

(1) Mnyama anayekufa peke yake damu yake haitoki, bali inakaa ndani ya nyama. Na sumu ambayo huwamo katika damu huingia mwilini mwa alaye nyama ile na kumdhuru afya yake.

(2) Pengine mnyama anakufa kwa ajili ya uzee na nyama yake haijengi mwili, maana *proteins* zake zimekwisha.

(3) Pengine mnyama anakufa kwa sumu au kuumwa na nyoka. Hivyo nyama yake ikiliwa inamwua mlaji. Tumesoma mara nyingi katika magazeti ya kwamba watu fulani wameambukizwa ugonjwa kwa sababu ya kula nyama ya ng'ombe aliyekufa, na wengine wao wakafa.

Damu ya wanyama na watu huwa na viini vya magonjwa mengi na ikiliwa inaharibu akili. Watu wanaochungua habari za vitu hivyo wanasema ya kwamba damu inaangamiza mishipa myepesi ya ubongo, na watu wanaotumia hawawezi kuvumbua mambo ya maarifa na elimu za

FUNGU 22

لَيْسَ الْبِرَّ اَنْ تُوَلُّوْا وُجُوْهَكُمْ قِبَلَ
الْمَشْرِقِ وَالْمَغْرِبِ وَلٰكِنَّ الْبِرَّ مَنْ اٰمَنَ
بِاللّٰهِ وَالْيَوْمِ الْاٰخِرِ وَالْمَلٰٓئِكَةِ وَالْكِتٰبِ
وَالنَّبِيّٖنَ ۚ وَاٰتَى الْمَالَ عَلٰى حُبِّهٖ ذَوِى
الْقُرْبٰى وَالْيَتٰمٰى وَالْمَسٰكِيْنَ وَابْنَ
السَّبِيْلِ ۙ وَالسَّآئِلِيْنَ وَفِى الرِّقَابِ ۚ

178. Si wema kuwa ninyi mwelekeze nyuso zenu upande wa mashariki na magharibi, bali wema hasa ni (wa yule) anayemwamini Allah na siku ya Mwisho na Malaika na Kitabu na Manabii, na anawapa mali - juu ya kuipenda - ndugu, na mayatima, na maskini, na msafiri na waombao, na katika (kuwakomboa) mateka, na

---

undani. Mtume *s.a.w.* alisema: Samaki ni halali kuliwa bila kuchinjwa, maana hana damu nyingi, tena ni mnyama wa majini. Damu inaweza kutumiwa kama ikiisha safishwa sana hata ikawa nyeupe na ukali na dhara yake ikaondolewa kabisa - ndiyo maziwa.

Nyama ya nguruwe.

(1) Imethibitika ya kwamba nyama ya nguruwe ina magonjwa maalumu kama tegu, mti na donda baya liitwalo *cancer* na *encysted trichina* na *trichinosis*, ambayo yapatikana katika watu wanaoila. Basi kuacha kula nyama ya nguruwe ni kujiepusha na magonjwa mengi.

(2) Nyama ya nguruwe inaleta joto jingi na inachafua mawazo ya binadamu. Inasemekana kwamba ndani ya nyama hii mna *exothermal proteins* nyingi zaidi, na kwa sababu hii inamfanya mtu kuvua nguo zake au kutaka kuzitoa hizo *proteins* kwa haraka sana na kwa njia hii anashawishika kuwa mfisadi.

(3) Nguruwe ana tamaa nyingi ya chakula na kuingiliana. Wanaotumia nyama yake wanapata tabia hiyo mbaya.

(4) Nguruwe hana ghera, hata hajali jike wake kupandwa na mwengine. Atakayetumia nyama yake pia atachukua tabia hiyo mbaya ya kutokuwa na ghera wala haya naye atavumilia mambo ya kishenzi yanayovumiliwa na nguruwe.

(5) Nguruwe anapenda sana kula vitu vichafu na kukaa matopeni na mahali pachafu. Waaminio wanaotakiwa kuwa na usafi wa moyo na mwili hawaruhusiwi kula nyama yake wasije wakachukuwa mienendo michafu ya nguruwe.

Kilichosomewa ghairi ya jina la Allah. Kimekatazwa kuliwa kwa sababu za kiroho. Mwenye kumpenda Allah hatatumia vitu vilivyotolewa sadaka kwa watu wengine au vilivyochinjwa kwa kufurahisha masanamu na miungu ya uwongo.

Basi, Waislamu wamekatazwa kutumia vitu hivyo, siyo kwa sababu Allah anataka kuwanyima riziki nzuri, bali makusudio yake hasa ni kulinda dini yao na afya yao na mienendo yao.

Isifahamiwe kwamba vitu vilivyotajwa katika Aya hii ndivyo hivyo tu vilivyokatazwa katika Sheria ya Kiislamu; maana vitu vilivyokatazwa ni namna nyingi: (1) *Haraam,* (2) *Mamnuu',* na (3) *Makruuh.* Vilivyobainishwa hapa ni vya namna ya kwanza, na Waislamu hawahitilafiani juu yao. Vitu vya namna nyingine mbili vimeelezwa katika hadithi za Mtume *s.a.w.* na vyuo vya Maimamu.

Aya 178. *'Alaa hubbihii.* Maneno haya mawili yanaweza kufasiriwa namna tatu: Ikiwa dhamiri (kijina) ya *hii* katika neno *hubbihii* inahusu mali, neno hili litafasiriwa "juu ya kuipenda."

anasimamisha Sala, na kutoa Zaka; na watekelezao ahadi zao wanapoahidi; na wavumiliao katika shida na dhara na katika wakati wa mapigano; hao ndio wasemao kweli, na hao ndio wamchao Mungu.

وَاَقَامَ الصَّلٰوةَ وَاٰتَى الزَّكٰوةَ ۚ وَالْمُوْفُوْنَ
بِعَهْدِهِمْ اِذَا عٰهَدُوْا ۚ وَالصّٰبِرِيْنَ فِي
الْبَاْسَآءِ وَالضَّرَّآءِ وَحِيْنَ الْبَاْسِ ؕ
اُولٰٓئِكَ الَّذِيْنَ صَدَقُوْا ؕ وَاُولٰٓئِكَ
هُمُ الْمُتَّقُوْنَ ﴿١٧٧﴾

179. Enyi mlioamini mmelazimishwa kisasi kuhusiana na waliouawa, mwungwana kwa mwungwana, na mtumwa kwa mtumwa, na mwanamke kwa mwanamke; lakini anayesamehewa na ndugu yake cho chote, basi ufuatiliaji (wa jambo hili kwa nia ya kuzipata fedha za malipo ya fidia) ni lazima ufanyike kwa uadilifu na (yule muuaji) ni lazima amlipe huyo nduguye hizo fedha za fidia kwa njia iliyo nzuri; hiyo ni tahafifu itokayo kwa Mola wenu, na ni rehema; na atakayeruka mipaka baada ya haya, basi yeye atapata adhabu iumizayo.

يٰٓاَيُّهَا الَّذِيْنَ اٰمَنُوْا كُتِبَ عَلَيْكُمُ الْقِصَاصُ
فِي الْقَتْلٰى ؕ اَلْحُرُّ بِالْحُرِّ وَالْعَبْدُ بِالْعَبْدِ
وَالْاُنْثٰى بِالْاُنْثٰى ؕ فَمَنْ عُفِيَ لَهٗ مِنْ اَخِيْهِ
شَيْءٌ فَاتِّبَاعٌ بِالْمَعْرُوْفِ وَاَدَآءٌ اِلَيْهِ
بِاِحْسَانٍ ؕ ذٰلِكَ تَخْفِيْفٌ مِّنْ رَّبِّكُمْ
وَرَحْمَةٌ ؕ فَمَنِ اعْتَدٰى بَعْدَ ذٰلِكَ فَلَهٗ
عَذَابٌ اَلِيْمٌ ﴿١٧٩﴾

180. Na mnao uzima katika kisasi enyi wenye akili, ili msalimike.

وَلَكُمْ فِي الْقِصَاصِ حَيٰوةٌ يّٰٓاُولِي
الْاَلْبَابِ لَعَلَّكُمْ تَتَّقُوْنَ ﴿١٨٠﴾

Yaani, ingawa anaipenda mali yake, lakini anaitoa kwa kuwapa nduguze na mayatima na wengine wenye haja, kama tulivyoiandika tafsiri hiyo hapo juu. (2) Na kama dhamiri hii ni ya Allah, neno hilo litafasiriwa "kwa kumpenda," yaani, mali hiyo mtu anaitoa si kwa kutafuta sifa mbele ya watu bali hasa kwa kumpenda Mola wake na kwa kufuata amri Yake. (3) Lakini kama dhamiri hii itarejeshwa kwenye neno *Aataa* basi itafasiriwa "kwa kupenda kutoa," yaani mtu mwema hatosheki na kutoa mali yake safari moja, bali amezoea kuitoa mali yake na anaitoa kwa sababu anapenda kuitoa.

Aya 179. *Mwungwana kwa mwungawa.* Hapa Allah Amevunja desturi moja mbovu iliyokuwa ikipatikana katika Waarabu. Kama mtumwa au mwanamke wa kabila fulani akimwua mtu wa kabila jingine, watu wa kabila lile wanasema sisi hatutaki kumwua mtumwa au mwanamke aliyeua, bali tutaua mwungwana au waungwana wengi, maana sisi tuna heshima zaidi. Basi hao Allah Amesema kuwa mwuaji tu ndiye atakayeuwawa, akiwa mwungwana au mtumwa au mwanamke.

Basi ufuatiliaji ni lazima ufanyike kwa uadilifu. Hii ina maana kwamba hizo fedha za malipo ya fidia ni lazima zikadiriwe kwa uadilifu na kwa njia nzuri na kisha zilipwe kwa ndugu wa yule mtu aliyeuawa.

Aya 180. *Mnao uzima katika kisasi enyi wenye akili.* Dini ya Kiislamu haikubali mtu ashambulie

كُتِبَ عَلَيْكُمْ اِذَا حَضَرَ اَحَدَكُمُ
الْمَوْتُ اِنْ تَرَكَ خَيْرَا ۖ الْوَصِيَّةُ
لِلْوَالِدَيْنِ وَالْاَقْرَبِيْنَ بِالْمَعْرُوْفِ ۚ
حَقًّا عَلَى الْمُتَّقِيْنَ ﴿١٨٠﴾

181. Mnalazimishwa, mmoja wenu anapofikiwa na mauti kama akiacha mali, kufanya wasia kwa wazazi na jamaa sawa na sheria: ndio wajibu kwa wamchao Mungu.

فَمَنْۢ بَدَّلَهٗ بَعْدَ مَا سَمِعَهٗ فَاِنَّمَاۤ اِثْمُهٗ عَلَى
الَّذِيْنَ يُبَدِّلُوْنَهٗ ؕ اِنَّ اللّٰهَ سَمِيْعٌ عَلِيْمٌ ﴿١٨١﴾

182. Lakini atakayeubadilisha (wasia) baada ya kuusikia, basi dhambi yake ni juu ya wale tu watakaoubadilisha; hakika Allah ndiye Asikiaye Ajuaye.

فَمَنْ خَافَ مِنْ مُّوْصٍ جَنَفًا اَوْ اِثْمًا
فَاَصْلَحَ بَيْنَهُمْ فَلَاۤ اِثْمَ عَلَيْهِ ؕ اِنَّ اللّٰهَ
غَفُوْرٌ رَّحِيْمٌ ﴿١٨٢﴾ ع ٢٢ ٦

183. Na anayehofia kwa muusiaji kwenda upande au dhambi, na akasuluhisha kati yao, basi hatakuwa na dhambi; hakika Allah ni Msamehevu Mrehemevu.

FUNGU 23

يٰۤاَيُّهَا الَّذِيْنَ اٰمَنُوْا كُتِبَ عَلَيْكُمُ الصِّيَامُ
كَمَا كُتِبَ عَلَى الَّذِيْنَ مِنْ قَبْلِكُمْ
لَعَلَّكُمْ تَتَّقُوْنَ ﴿١٨٣﴾

184. Enyi mlioamini, mmelazimishwa kufunga Saumu kama walivyolazimishwa wa kabla yenu ili mpate kumcha Mungu.

mwenzake pasina sababu. Akifanya hivyo na kuuwa basi naye pia auwawe. Linganisha fundisho hili lenye thamani na fundisho la Injili inaposema, "Msishindane na mtu mwovu. Kama mtu anakupiga shavu la kuume, mwelekezee la pili. Kama mtu anataka kushindana nawe katika hukumu na kukutoza kanzu yako, mwachilie na joho vile vile." (Matei 5:39, 40).

Fundisho hilo la Injili linapendeza masikioni na pengine mhubiri pia anaweza kusifiwa na wasikilizaji wake, lakini hapajawa na serikali yo yote iliyofuata amri hii kisha ikastawi na kufaulu kuleta amani duniani. Serikali ya Kikristo hasa ndiyo ya kwanza kuua mwuaji na kuadhibu mhalifu. Na kama ingevumilia uasi na uuaji isingeendelea kwa muda mrefu. Kwa ajili hii Allah alipoeleza amri ya kulipiza kisasi, alitaka watu watumie akili yao na kufikiri, je, kumwua mwuaji mmoja ni bora au kuacha watu wote katika hali ya kutosalimika. Kweli amri hii ya Qur'an kufuatwa ndiyo amani inaweza kuwapo duniani.

Aya 181. Habari za wasia na taratibu ya sehemu za mali ya maiti zimeelezwa pahali pengine katika Qur'an (sura Nisaa). Hapa Allah anaeleza habari za wazazi na jamaa wengine wasioweza kupata urithi kwa Sheria ya Kiislamu. Basi, Allah anasema kuwa watu wa namna hiyo wafanyiwe hisani, na afadhali mtu awafanyie wasia wapewe sehemu fulani ya mali. Kwa mfano: baba mzazi anayo sehemu yake maalumu katika urithi. lakini ikiwa yeye si Mwislamu, hawezi kupata urithi. Basi, katika hali ya namna hii ni vizuri afanyiwe wasia.

Aya 184. Amri ya kufunga saumu inapatikana katika dini karibu zote ingawa kanuni zake zimehitilafiana. Saumu aliyofunga Budha (Lalitavistara na Buddhacharita), Saumu aliyofunga Musa kabla hajapewa amri kumi (Kutoka 34:28; Kumbukumbu 9:9), Saumu aliyofunga Yesu kabla hajapewa kazi ya Utume (Matt. 4:2) na maagizo ya kufunga aliyowaeleza wafuasi wake

(Matt. 6:16, 18), yote hayo yanaonyesha jinsi Saumu ilivyo ni jambo la maana sana. Wanazuoni wa Ulaya wameandika, "Dini nyingi zaidi, katika ustaarabu wa chini, na katika wa juu zimeagiza kufunga saumu, na inapokuwa haikuagizwa, hata hivyo watu wenyewe hujifungia kwa kushawishiwa na silika ya kiasili" (Encyclopaedia Britannica).

Lakini Aya hii haisemi kuwa Waislamu wameagizwa kufunga kwa namna ile ile waliyoambiwa watu wa zamani. Islam imeikuza vema desturi hii ya kufunga saumu kwa kuiwekea kanuni zenye manufaa na vizuizi pia.

Ili mpate kumcha Mungu. Kifungu hiki cha Maneno kinaeleza hekima kubwa inayofungamana na saumu. Ni desturi ya Qur'an inapotoa amri yenye maana, papo kwa papo inaeleza faida yake ili mtu ajue na atosheke na hekima ya kupewa amri hiyo. Katika kifungu hicho kusudi la Saumu limeelezwa

kuwa ni kupata *Taq-waa,* yaani, ucha-Mungu. Neno *Taq-waa,* linatumiwa katika Qur'an kwa maana tatu: (1) Kuepukana na maumivu, (2) kuepukana na dhambi, (3) kufikia utakatifu ulio juu wa mambo ya kiroho.

Kufunga Saumu kunatoa mambo yote hayo matatu. Kwa mara ya kwanza maelezo haya yanaonekana yenye kukanganya, kusema ya kwamba kufunga Saumu kunamhifadhi mtu na maumivu, kwani kufunga kwenyewe kunamtia mtu kadiri fulani ya maumivu. Lakini tukifikiri kidogo tutaona ya kwamba kufunga Saumu kunawafunza watu somo linaloleta manufaa juu ya taifa lao.

(1) Somo la kwanza ni hili ya kwamba, tajiri ambaye hajaona uchungu wa njaa wala kupungukiwa hawezi kutambua taabu za nduguze walio maskini ambao mara nyingi wamekaa bila chakula. Lakini yeye mwenyewe anapofunga, anatambua njaa ni kitu gani na aweza kufikiria yote yanayowasibu maskini. Hivyo anaanza kuwahurumia maskini, na matokeo yatakuwa kuongezeka hali njema za taifa zima.

(2) Sababu nyingine ya kufunga ni kuwa Islam haitaki wafuasi wake wawe wazembe na wavivu na wasioelekea kuvumilia taabu. Bali inawataka wawe tayari na wenye uwezo wa kupokea kila namna ya upungufu na shida katika wakati wa taabu. Saumu zinawafanya Waislamu kuwa na tabia za kuvumilia njaa na kiu na kujizuia nafsi zao katika mahitaji na shauku, na hao wanaoifuata amri hii kwa uaminifu sana hawawi wavivu kamwe, wala hawawi wenye kujiendekeza.

(3) Tena Saumu inamhifadhi mtu na dhambi, maana dhambi huzalika katika kupenda starehe za kimwili. Mtu anapokuwa amezoea tabia fulani inamwia shida sana kuiacha. Lakini mtu ambaye anaweza kuachilia mbali tabia au mwenendo po pote anapotaka, kamwe hawezi kutawaliwa nao. Mtu anayeacha furaha zote za mwili ambazo mara kwa mara zinamvutia kwenye dhambi, kwa mwezi mzima ili apate radhi ya Allah, na anajifunza kujitawala na kujizuia, anaweza kuyashinda kwa urahisi majaribio ya kutenda dhambi.

(4) Tena, kama ilivyo katika mwezi wa kufunga Saumu, mtu yampasa kuamka katika saa za mwisho wa siku kwa kula daku, hapo anapata nafasi zaidi ya kuomba na kuabudu, ambayo humwongoza upesi kwenye njia ya maendeleo ya kiroho, na anapoitoa starehe na faraja yake sadaka kwa Mwenyezi Mungu, basi Allah Anaitia nguvu roho yake na kumvuta awe karibu naye.

Baki ya Saumu ya mwezi mzima wa Ramadhani ambayo ni ya lazima, mtu anaweza pia kufunga Saumu katika siku zingine Kufunga siku ya Ijumaa peke yake, imekatazwa, isipokuwa mtu afunge Ijumaa na Jumamosi, au Alhamisi na Ijumaa. Kadhalika kufunga siku za Idi imekatazwa.

Mtume *s.a.w.* alisema, "Mtu anayefunga Ramadhani, kisha akafunga siku sita za mwezi Shawwaal (Mfunguo mosi), yeye ni kama amefunga mwaka mzima" (Muslim). Kadhalika Mtume *s.a.w.* akasema, "Mtu anayefunga siku moja kwa ajili ya Allah, basi Mungu atamweka mbali na Moto kwa umbali wa miaka sabini" (Muslim). Baadhi ya Saumu zilizo suna ni kufunga siku ya Arafa, yaani tarehe 9 Mfunguo tatu, na kufunga siku tatu katika kila mwezi.

Watoto wadogo hawaruhusiwi kufunga. Kadhalika si ruhusa kwa mtu kufunga siku zote bila kuacha. Mtume *s.a.w.* akasema, "Kwa hakika mimi ni mchaji zaidi kuliko ninyi, lakini wakati mwingine nafunga na wakati mwingine sifungi, basi nanyi mfanye hivyo". (Bukhari).

185. Kwa siku zilizohesabiwa. Lakini miongoni mwenu awaye mgonjwa au katika safari, basi atimize hesabu katika siku zingine. Na wale wanaoweza, watoe fidia kwa kumlisha maskini. Na atakayefanya wema kwa radhi ya nafsi yake, basi ni bora kwake; na kama mkifunga ni bora kwenu, ikiwa mnajua.

اَيَّامًا مَّعْدُوْدٰتٍ ؕ فَمَنْ كَانَ مِنْكُمْ
مَّرِيْضًا اَوْ عَلٰى سَفَرٍ فَعِدَّةٌ مِّنْ اَيَّامٍ
اُخَرَ ؕ وَعَلَى الَّذِيْنَ يُطِيْقُوْنَهٗ فِدْيَةٌ
طَعَامُ مِسْكِيْنٍ ؕ فَمَنْ تَطَوَّعَ خَيْرًا فَهُوَ
خَيْرٌ لَّهٗ ؕ وَاَنْ تَصُوْمُوْا خَيْرٌ لَّكُمْ اِنْ
كُنْتُمْ تَعْلَمُوْنَ ﴿١٨٥﴾

186. Mwezi wa Ramadhani ambao imeteremshwa humo Qur'an kuwa mwongozo kwa watu, na Ishara zilizo wazi za mwongozo na kipambanuzi. Basi miongoni mwenu atakayeuona mwezi, afunge saumu, na mwenye kuwa mgonjwa au yumo safarini, basi atimize hesabu katika siku zingine. Allah Huwatakieni yaliyo mepesi wala Hawatakieni yaliyo mazito, na pia (Huwatakieni) mtimize hesabu na kumtukuza Allah kwa kuwa Amewaongozeni, na ili mpate kushukuru.

شَهْرُ رَمَضَانَ الَّذِيْٓ اُنْزِلَ فِيْهِ الْقُرْاٰنُ
هُدًى لِّلنَّاسِ وَبَيِّنٰتٍ مِّنَ الْهُدٰى
وَالْفُرْقَانِ ۚ فَمَنْ شَهِدَ مِنْكُمُ الشَّهْرَ
فَلْيَصُمْهُ ؕ وَمَنْ كَانَ مَرِيْضًا اَوْ عَلٰى سَفَرٍ
فَعِدَّةٌ مِّنْ اَيَّامٍ اُخَرَ ؕ يُرِيْدُ اللّٰهُ بِكُمُ
الْيُسْرَ وَلَا يُرِيْدُ بِكُمُ الْعُسْرَ ۖ
وَلِتُكْمِلُوا الْعِدَّةَ وَلِتُكَبِّرُوا اللّٰهَ عَلٰى مَا
هَدٰىكُمْ وَلَعَلَّكُمْ تَشْكُرُوْنَ ﴿١٨٦﴾

Aya 185. *Na wale wanaoweza , watoe fidia.* Maneno haya yanaeleza habari za watu walio wazee sana, au wanawake wanaonyonyesha watoto wao, au wenye mimba au watu wasio na afya nzuri. Yaani kufunga wangeweza kufunga, lakini jambo hili litawatia katika taabu isiyovumilika. Basi watu wa namna hii wasifunge, bali watoe fidia kwa kumlisha maskini chakula sawa na chakula wanachotumia wenyewe kwa muda wa siku za Saumu.

Aya 186. *Mungu Huwatakieni yaliyo mepesi.* Ndiyo kusema ya kwamba amri za Allah haziletwi ili kuwataabisha watu, bali kuwapa raha na faraja. Lakini Padre Dale anadhani ya kuwa mtu aliyeacha kufunga kwa ugonjwa na safari, kulipa fidia ya Saumu yake, au kuifunga baadaye, ni kumbebesha mizigo miwili. Mwislamu hafikiri kuwa amri hizo ni taabu, maana kuna Waislamu ambao wako radhi kufunga na ugonjwa na katika safari, na wanafanya hivyo kwa shauku sana ingawa Sheria haitaki wafanye hivyo. Kadhalika kuna Waislamu waliofunga saa 24 kwa furaha ingawa Sheria haikuwataka na inawakataza kufanya hivyo. Kwa hiyo kufunga baada ya ugonjwa na safari au kulipa fidia Mwislamu haoni kuwa ni mizigo miwili, bali anaona ni nafuu mbili. Maana Mtume s.a.w. amesema, kila taabu anayopata Mwislamu, hata kuchomwa na mwiba, inafanya afutiwe katika madhambi yake (Bukhari).

Haoni taabu kwa hayo ila padre anayegalagala katika starehe na anasa za dunia na bado anajidhani ndiyo kumcha Mungu. Kwake Sheria ya Mungu ni "laana" na "kunaswa katika kongwa la utumwa" (Wagalatia 3:13 na 5:1).

187. Na waja wngu wakuulizapo juu Yangu, basi hakika Mimi Nipo karibu. Nayaitika maombi ya mwombaji ana-poniomba, basi waniitikie na waniamini, ili wapate kuongoka.

وَ اِذَا سَاَلَكَ عِبَادِیْ عَنِّیْ فَاِنِّیْ قَرِیْبٌ ؕ
اُجِیْبُ دَعْوَةَ الدَّاعِ اِذَا دَعَانِ ۙ
فَلْیَسْتَجِیْبُوْا لِیْ وَلْیُؤْمِنُوْا بِیْ لَعَلَّهُمْ
یَرْشُدُوْنَ ﴿۱۸۷﴾

188. Mmehalalishiwa usiku wa Saumu kuingiliana na wake zenu. Wao ni nguo kwenu na ninyi ni nguo kwao. Allah Amekwisha jua ya kwamba mlikuwa mkijihini nafsi zenu, kwa hiyo amewaelekeeni na kuwasameheni; basi sasa laleni nao na takeni Aliyowaandikieni Allah. Na kuleni na kunyweni mpaka ubainike kwenu uzi mweupe kutoka katika uzi mweusi wa alfajiri, kisha timizeni Saumu mpaka usiku. Wala msilale nao na hali mnakaa misikitini; hiyo ndiyo mipaka ya Allah, basi msiikaribie. Hivi ndivyo Allah Anavyobainisha aya Zake kwa watu ili wapate kumcha.

اُحِلَّ لَكُمْ لَیْلَةَ الصِّیَامِ الرَّفَثُ اِلٰی
نِسَآئِكُمْ ؕ هُنَّ لِبَاسٌ لَّكُمْ وَاَنْتُمْ لِبَاسٌ
لَّهُنَّ ؕ عَلِمَ اللّٰهُ اَنَّكُمْ كُنْتُمْ تَخْتَانُوْنَ
اَنْفُسَكُمْ فَتَابَ عَلَیْكُمْ وَعَفَا عَنْكُمْ ۚ
فَالْـٰٔنَ بَاشِرُوْهُنَّ وَابْتَغُوْا مَا كَتَبَ اللّٰهُ
لَكُمْ ۪ وَكُلُوْا وَاشْرَبُوْا حَتّٰی یَتَبَیَّنَ لَكُمُ
الْخَیْطُ الْاَبْیَضُ مِنَ الْخَیْطِ الْاَسْوَدِ مِنَ
الْفَجْرِ ۪ ثُمَّ اَتِمُّوا الصِّیَامَ اِلَی الَّیْلِ ۚ وَلَا
تُبَاشِرُوْهُنَّ وَاَنْتُمْ عٰكِفُوْنَ ۙ فِی
الْمَسٰجِدِ ؕ تِلْكَ حُدُوْدُ اللّٰهِ فَلَا
تَقْرَبُوْهَا ؕ كَذٰلِكَ یُبَیِّنُ اللّٰهُ اٰیٰتِهٖ
لِلنَّاسِ لَعَلَّهُمْ یَتَّقُوْنَ ﴿۱۸۷﴾

189. Wala msiliane mali zenu kwa batili na kuzipeleka (kama hongo) kwa mahakimu ili mpate kula sehemu ya mali ya watu (wengine) kwa dhambi na hali mnajua.

وَلَا تَاْكُلُوْٓا اَمْوَالَكُمْ بَیْنَكُمْ بِالْبَاطِلِ
وَتُدْلُوْا بِهَآ اِلَی الْحُكَّامِ لِتَاْكُلُوْا فَرِیْقًا
مِّنْ اَمْوَالِ النَّاسِ بِالْاِثْمِ وَاَنْتُمْ
تَعْلَمُوْنَ ﴿۱۸۸﴾ ع ۲۳ ۶ ۷

Aya 187. *Mimi Nipo karibu.* Siyo maana yake kuwa Mungu anao mwili, zamani alikuwa mbali na sasa amesogea karibu, hasha. Bali kusudi la kusema "Mimi Nipo karibu" ni kueleza kuwa amtafutaye Allah kwa mapenzi na unyenyekevu atapata rehema yake upesi, na maombi yake yatapokelewa.

Aya 188. *Wao ni nguo kwenu.* Mwanamke hajapewa heshima ya namna hii katika dini yo yote. Mwanamume anaambiwa kuwa yeye ni uchi pasipo mkewe, na mke ni uchi pasipo mumewe, yaani heshima yao inategemeana. Kama hawataheshimiana wote wawili watapoteza heshima yao. Nguo ni sababu ya raha na mapambo. Lazima mume awe sababu ya raha na mapambo kwa ajili ya mkewe na mke awe sababu ya raha na mapambo kwa ajili ya mumewe.

Mlikuwa mkijihini nafsi zenu. Mayahudi walikuwa wakifunga Saumu ya saa 24. Waislamu walipoambiwa kufunga, wakaanza kufuata mwendo ule ule wa Mayahudi, yaani, kama mtu

FUNGU 24

190. Wanakuuliza juu ya miezi, Sema: Hiyo ni vipimo vya nyakati kwa ajili ya watu na kwa Haji. Na si wema kuyaingia majumba kwa nyuma yao, bali wema hasa ni wa yule anayemcha. Na ingieni majumbani kwa kupitia milangoni mwao, na mcheni Allah ili mpate kufaulu.

يَسْـَٔلُوْنَكَ عَنِ الْاَهِلَّةِ ؕ قُلْ هِيَ مَوَاقِيْتُ لِلنَّاسِ وَالْحَجِّ ؕ وَلَيْسَ الْبِرُّ بِاَنْ تَاْتُوا الْبُيُوْتَ مِنْ ظُهُوْرِهَا وَلٰكِنَّ الْبِرَّ مَنِ اتَّقٰى ۚ وَاْتُوا الْبُيُوْتَ مِنْ اَبْوَابِهَا ۪ وَاتَّقُوا اللّٰهَ لَعَلَّكُمْ تُفْلِحُوْنَ ﴿۱۸۹﴾

191. Na piganeni katika njia ya Allah na wale wanaowapigeni, wala msiruke mipaka. Kwa yakini Allah hawapendi warukao mipaka.

وَقَاتِلُوْا فِيْ سَبِيْلِ اللّٰهِ الَّذِيْنَ يُقَاتِلُوْنَكُمْ وَلَا تَعْتَدُوْا ؕ اِنَّ اللّٰهَ لَا يُحِبُّ الْمُعْتَدِيْنَ ﴿۱۹۰﴾

---

amewahi kwenda kitandani na kulala kidogo anaacha kabisa kula, kunywa na kuingiliana na mkewe (Bukhari) Na hivyo Masahaba wa Mtume *s.a.w.* wakajitaabisha wenyewe, pasi kuwa na amri ya Mungu. Basi Mungu hakutaka hivyo na akaleta aya hiyo ya juu, na akawaambia kuwa wanaweza kula, kunywa na kuingiliana mpaka mapambazuko.

Aya hii inaonyesha ya kwamba toka mapambazuko mpaka jua kuchwa Waislamu waache kula, kunywa na kuingiliana maadamu wamefunga Saumu. Na wanaruhusiwa kufanya hayo yote baada ya jua kutua mpaka kabla ya mapambazuko ya alfajiri. Katika nchi ambazo usiku na mchana ni virefu kuliko desturi, yaani karibu na ncha mbili za dunia, kaskazini na kusini, basi huko wanaofunga watahesabu Saumu zao kwa saa. Usiku utahesabiwa saa kumi na mbili na mchana pia. (Muslim).

Hali mnakaa misikitini. Maneno haya yanahusu desturi iitwayo *I'tikaaf* ya kukaa usiku na mchana msikitini bila kutoka isipokuwa kwa haja za lazima kama kwenda choo. Huingia msikitini tarehe 20 ya Ramadhani na kukaa humo humo mpaka mwisho wa mwezi, akiendelea na Saumu zake na akijishughulisha na maombi na kusoma Qur'an au vitabu vingine vya dini au kumkumbuka Allah na kufikiria sifa Zake. Katika *I'tikaaf* kuingiliana na wake na mambo yanayopelekea huko haijuzu hata kama ni usiku.

Uzi mweupe katika uzi mweusi. Si mradi wake uzi wa pamba au wa katani, bali mradi ni ule weupe wa asubuhi na weusi wa usiku.

Aya 189. Hapa neno (wengine) laonekana kuwa halina ulazima wa kutumika kwa vile aya hii yaonekana kuwa kimsingi inhusika na fedha za umma na mali ya taifa.

Aya 190. *Wanakuuliza juu ya miezi.* Masahaba walipojua habari za baraka za mwezi wa Ramadhani walitaka kujua fadhila za miezi mingine pia.

Aya 191. *Piganeni ..... na wale wanaowapigeni.* Aya hii inaeleza asili ya vita zote za dini ya Kiislamu: (1) Kupigana katika njia ya Allah ili kuondoa vizuizi vilivyotiwa na watu katika njia ya Allah, na vita isiwe kwa ajili ya dunia. (2) Ni ruhusa kupigana na wale tu wanaochukua silaha mbele ili kuuangamiza Uislamu. (3) Wasipigane na wale wasiopigana nao, kama wazee, watoto, wanawake, watu wa dini na watu wasiowasaidia wapiganano. (Abu Dawud). (4) Vita isizidi kiasi, mara adui aachapo kupigana Waislamu pia waache.

192. Na wauweni (vitani) po pote mwakutapo, na kuwatoa po pote walipokutoeni; kwani mateso ni mabaya zaidi kuliko kuua. Wala msipigane nao karibu na Msikiti Mtakatifu mpaka wawapigeni ndani yake. Na wakiwapigeni basi nanyi pia wapigeni: kama hivyo ndiyo malipo ya makafiri.

وَاقْتُلُوْهُمْ حَيْثُ ثَقِفْتُمُوْهُمْ
وَاَخْرِجُوْهُمْ مِّنْ حَيْثُ اَخْرَجُوْكُمْ
وَالْفِتْنَةُ اَشَدُّ مِنَ الْقَتْلِ ۚ وَلَا
تُقٰتِلُوْهُمْ عِنْدَ الْمَسْجِدِ الْحَرَامِ حَتّٰى
يُقٰتِلُوْكُمْ فِيْهِ ۚ فَاِنْ قٰتَلُوْكُمْ
فَاقْتُلُوْهُمْ ؕ كَذٰلِكَ جَزَآءُ الْكٰفِرِيْنَ ﴿۱۹۱﴾

193. Lakini kama wakiacha, basi hakika Allah ni Msamehevu, Mrehemevu.

فَاِنِ انْتَهَوْا فَاِنَّ اللّٰهَ غَفُوْرٌ رَّحِيْمٌ ﴿۱۹۲﴾

194. Na wapigeni mpaka pasiwe mateso, na dini iwe kwa ajili ya Allah tu; na kama wakiacha, basi usiweko uadui ila kwa wadhalimu.

وَقٰتِلُوْهُمْ حَتّٰى لَا تَكُوْنَ فِتْنَةٌ وَّيَكُوْنَ
الدِّيْنُ لِلّٰهِ ؕ فَاِنِ انْتَهَوْا فَلَا عُدْوَانَ
اِلَّا عَلَى الظّٰلِمِيْنَ ﴿۱۹۳﴾

195. Mwezi mtakatifu kwa mwezi mtakatifu, na vitu vitakatifu vimewekewa kisasi. Na anayewashambulieni, nanyi pia mumshambulie, kwa kadiri alivyowashambulieni, na Mwogopeni Allah, na jueni ya kwamba Allah Yu pamoja na wamchao.

اَلشَّهْرُ الْحَرَامُ بِالشَّهْرِ الْحَرَامِ
وَالْحُرُمٰتُ قِصَاصٌ ؕ فَمَنِ اعْتَدٰى
عَلَيْكُمْ فَاعْتَدُوْا عَلَيْهِ بِمِثْلِ مَا اعْتَدٰى
عَلَيْكُمْ ۪ وَاتَّقُوا اللّٰهَ وَاعْلَمُوْٓا اَنَّ اللّٰهَ
مَعَ الْمُتَّقِيْنَ ﴿۱۹۴﴾

Aya 194. *Mpaka pasiwe mateso.* Neno mateso maana yake mateso kwa ajili ya dini. Yaani Waislamu wanaweza kupigana na makafiri mpaka waache kuwatesa kwa ajili ya dini, na kila mtu awe na hiari ya kukubali dini anayoipenda.

Dini iwe kwa ajili ya Allah. Watu waweze kukubali dini kwa uhuru, siyo kuwa wakubali dini yo yote kwa kuogopa kuteswa na watu. Mataifa ya U.N.O. yamekwisha tangaza kuwa watu ni huru kufuata dini yo yote waitakayo. Sifa ni ya dini ya Kiislamu iliyosimamisha toka zamani kanuni hii.

Aya 195. *Mwezi mtakatifu kwa mwezi mtakatifu.* Toka zamani miezi minne ya mwaka, yaani *Dhul-Qaada, Dhul-Hijja, Al-Muharram* na *Rajabu* ilifahamiwa miezi mitakatifu, na ilikuwa haramu kupigana katika miezi hiyo. Lakini juu ya hayo makabila mengine yakawashambulia Waislamu katika miezi hiyo. Basi, Waislamu wanaambiwa ya kuwa kama mkishambuliwa katika miezi mitakatifu, ninyi pia mnaweza kupigana, maana hii tu ndiyo njia ya kuulinda utukufu wa miezi hiyo.

196. Na toeni katika njia ya Allah, wala msijitupe kwa mikono yenu katika maangamizo, na fanyeni wema, hakika Allah huwapenda wafanyao wema.

وَاَنْفِقُوْا فِيْ سَبِيْلِ اللّٰهِ وَلَا تُلْقُوْا
بِاَيْدِيْكُمْ اِلَى التَّهْلُكَةِ ۛ وَاَحْسِنُوْا ۛ
اِنَّ اللّٰهَ يُحِبُّ الْمُحْسِنِيْنَ ﴿١٩٥﴾

197. Na timizeni Haji na Umra kwa ajili ya Allah; na kama mkizuiwa, basi (pelekeni) dhabihu yo yote mwezayo kuipata, wala msinyoe vichwa vyenu mpaka dhabihu ifike machinjioni pake; lakini miongoni mwenu awaye mgonjwa au ana maradhi kichwani mwake, basi atoe fidia kwa kufunga saumu au kutoa sadaka au kuchinja wanyama. Na mtakapokuwa salama, basi mwenye kujifaidisha kwa kufanya Umra pamoja na Haji, (atoe) dhabihu yo yote awezayo kuipata; lakini asiyepata, afunge saumu siku tatu katika Haji na siku saba mtakaporudi; hizi ni kumi kamili. Hayo ni kwa ajili ya yule ambaye ahali zake hawako karibu na Msikiti Mtakatifu. Na mcheni Allah na jueni kuwa Allah ni Mkali wa kuadhibu.

وَاَتِمُّوا الْحَجَّ وَالْعُمْرَةَ لِلّٰهِ ۭ فَاِنْ
اُحْصِرْتُمْ فَمَا اسْتَيْسَرَ مِنَ الْهَدْيِ ۚ
وَلَا تَحْلِقُوْا رُءُوْسَكُمْ حَتّٰى يَبْلُغَ
الْهَدْيُ مَحِلَّهٗ ۭ فَمَنْ كَانَ مِنْكُمْ مَّرِيْضًا
اَوْ بِهٖٓ اَذًى مِّنْ رَّاْسِهٖ فَفِدْيَةٌ مِّنْ صِيَامٍ
اَوْ صَدَقَةٍ اَوْ نُسُكٍ ۚ فَاِذَآ اَمِنْتُمْ ۣ
فَمَنْ تَمَتَّعَ بِالْعُمْرَةِ اِلَى الْحَجِّ فَمَا
اسْتَيْسَرَ مِنَ الْهَدْيِ ۚ فَمَنْ لَّمْ يَجِدْ
فَصِيَامُ ثَلٰثَةِ اَيَّامٍ فِي الْحَجِّ وَسَبْعَةٍ اِذَا
رَجَعْتُمْ ۭ تِلْكَ عَشَرَةٌ كَامِلَةٌ ۭ ذٰلِكَ
لِمَنْ لَّمْ يَكُنْ اَهْلُهٗ حَاضِرِي الْمَسْجِدِ
الْحَرَامِ ۭ وَاتَّقُوا اللّٰهَ وَاعْلَمُوْٓا اَنَّ اللّٰهَ
شَدِيْدُ الْعِقَابِ ﴿١٩٦﴾ ع

Aya 196. *Toeni katika njia ya Allah.* Katika vita zinatumika mali nyingi, na ni wazi kuwa kama makafiri washambulie kwa nguvu, na waaminio wasitoe mali kwa kujiweka tayari na kujilinda, bila shaka wataangamia. Leo hakuna vita vya dini lakini Jihadi ya kalamu na maneno iko, basi Waislamu watoe mali zao katika njia hii au sivyo mwisho watakumbwa na hatari kubwa.

Aya 197. *Timizeni Haji na Umra.* Haji ni nguzo ya mwisho katika nguzo tano za dini ya Kiislamu. Inamlazimu kila Mwislamu huru, balehe na mzima, kuhiji Makka mara moja katika maisha yake akiwa na mali ya kutosha na hapana hatari yo yote njiani.

Jambo la kwanza linalotakiwa katika Haji ni *Ihraam,* yaani kuvaa shuka mbili tu zisizoshonwa, Mhaji anakaa katika shuka hizo mpaka atimize Haji na Umra.

Jambo la pili ni *Tawaaf*, yaani; kuzunguka Kaaba mara saba, mara tatu mbio, na mara nne kwa kutembea.

Jambo la tatu ni kukimbia katikati ya vilima viwili, Safaa na Marwa, mara saba. Mhaji anaanza kukimbia toka kilima cha Safaa.

FUNGU 25

198. Haji (hufanyika ndani ya) miezi maalumu: na anayekusudia kufanya Haji katika (miezi) hiyo, basi asiingiliane wala asitukane wala asibishane katika Haji; na heri yo yote mnayoifanya, Allah Huijua; na chukueni masurufu, na hakika masurufu bora ni ucha-Mungu; na Nicheni Mimi enyi wenye akili.

اَلْحَجُّ اَشْهُرٌ مَّعْلُوْمٰتٌ ۚ فَمَنْ فَرَضَ
فِيْهِنَّ الْحَجَّ فَلَا رَفَثَ وَلَا فُسُوْقَ ۙ وَلَا
جِدَالَ فِي الْحَجِّ ۭ وَمَا تَفْعَلُوْا مِنْ خَيْرٍ
يَّعْلَمْهُ اللّٰهُ ۭ وَتَزَوَّدُوْا فَاِنَّ خَيْرَ الزَّادِ
التَّقْوٰى ۡ وَاتَّقُوْنِ يٰٓاُولِي الْاَلْبَابِ ۝۱۹۷

Jambo la mwisho ni kuhudhuria mkutano wa Mahaji katika uwanja wa 'Arafaat tarehe tisa ya mwezi wa Dhul-Hijja.

Kutimiza mambo hayo manne ni Haji, na kutimiza matatu ya kwanza na kuvua shuka za *Ihraam* ndiyo Umra. Umra inaweza kufanywa katika siku zozote za mwaka, lakini Haji ni katika siku zake maalumu.

FAIDA YA HAJI

Haji inaonyesha daraja ya mwisho katika kumpenda Allah. Mhaji anaacha nchi yake, jamaa zake, tabia zake mbaya na nguo zake za fahari na heshima, na anafika kwenye Nyumba Tukufu ya Allah kama maskini. Anayehiji kwa ajili ya Allah tu pasipo makusudio mengine yo yote, anasamehewa dhambi zote alizofanya. Mtume *s.a.w.* alisema, Mhaji anafanana na mtoto mchanga asiye na dhambi yo yote (Bukhari na Muslim).

Basi, desturi hizo zinazohusika na Haji ni desturi zenye maana sana ambazo zinamfunza Mwislamu ajiweke tayari kuviacha vyote vilivyomo duniani na kuitafuta radhi ya Mola wake. Hali ya *Ihraam* pia inamkumbusha siku ya kufufuliwa, na kumfanya asijali maisha ya dunia.

Na kama mkizuiwa. Kama vitokee vizuizi na mtu azuilike njiani kwa maradhi, vita, au kizuizi kingine, basi katika hali ya namna hii ni lazima kuchinja sadaka ya mbuzi, kondoo, ng'ombe au ngamia. Na mtu akae katika hali ya *Ihraam* mpaka sadaka ifike Makka pahali pa kuchinjia. Kama asiweze kupeleka hata sadaka zake mpaka Makka, basi anaweza kuzichinja po pote azuilikapo.

Awaye mgonjwa. Yaani mtu asiyeweza kunyoa kwa sababu ya maradhi au kwa sababu ya taabu zingine za kichwa yeye anaambiwa kufunga, au kuwalisha maskini au kuchinja sadaka, kadiri ya uwezo wake.

Mwenye kujifaidisha kwa kufanya Umra pamoja na Haji. Haji na Umra huweza kufanywa pamoja katika *Ihraam* moja. Inajuzu pia kufunga *Ihraam* ya Haji peke yake. Mwenye kupumzika hivyo anatakiwa kutoa sadaka. Sadaka hutolewa tena baada ya kutimiza Haji, mhaji anapofika Minaa kutoka 'Arafaat, tarehe 10.

Aya 198. Miezi ya kuhiji inajulikana sana nayo ni *Shawwaal, Dhul-Qaada,* na siku kumi za mwanzo wa mwezi wa *Dhul-Hijja.*

Asiingiliane wala asitukane wala asibishane. Maneno na mambo yote yanayohusu kuingiliana na wake, matusi na matukano, ubishi na ugomvi wa kila namna vimekatazwa kabisa katika Haji, kusudi mtu apate somo kubwa la kukaa kwa adabu nzuri katika siku zingine.

Masurufu bora ni ucha-Mungu. Anayeazimia kwenda kuhiji Makka ameamrishwa kuchukua masurufu yanayohitajika njiani kwa sababu watu wengine hawachukui masurufu ya kuwatosha kisha wanasumbuka ovyo. Katika maneno "masurufu bora" mhaji anaambiwa kuangalia usafi wa nia yake na unyofu wa moyo pia, asishughulike na kukusanya matumizi tu ilhali roho yake inabaki chafu. Utawa ndio masurufu bora yanayohitajika sana katika mambo yote ya ibada.

لَيْسَ عَلَيْكُمْ جُنَاحٌ اَنْ تَبْتَغُوْا فَضْلًا مِّنْ
رَّبِّكُمْ ؕ فَاِذَآ اَفَضْتُمْ مِّنْ عَرَفٰتٍ
فَاذْكُرُوا اللّٰهَ عِنْدَ الْمَشْعَرِ الْحَرَامِ ۠
وَاذْكُرُوْهُ كَمَا هَدٰىكُمْ ۚ وَاِنْ كُنْتُمْ
مِّنْ قَبْلِهٖ لَمِنَ الضَّآلِّيْنَ ﴿۱۹۸﴾

199. Si aibu kwenu kuitafuta fadhili ya Mola wenu; na mtakaporudi kutoka 'Arafati, basi Mkumbukeni Allah penye Mash'aril Haraam. Na Mkumbukeni kama Alivyowaongozeni, na ingawa zamani mlikuwa miongoni mwa waliopotea.

ثُمَّ اَفِيْضُوْا مِنْ حَيْثُ اَفَاضَ النَّاسُ
وَاسْتَغْفِرُوا اللّٰهَ ؕ اِنَّ اللّٰهَ غَفُوْرٌ رَّحِيْمٌ ﴿۱۹۹﴾

200. Kisha rudini toka mahali warudiapo watu, na ombeni msamaha kwa Allah, hakika Allah ni Msamehevu, Mrehemevu.

فَاِذَا قَضَيْتُمْ مَّنَاسِكَكُمْ فَاذْكُرُوا اللّٰهَ
كَذِكْرِكُمْ اٰبَآءَكُمْ اَوْ اَشَدَّ ذِكْرًا ؕ فَمِنَ
النَّاسِ مَنْ يَّقُوْلُ رَبَّنَآ اٰتِنَا فِى الدُّنْيَا وَمَا
لَهٗ فِى الْاٰخِرَةِ مِنْ خَلَاقٍ ﴿۲۰۰﴾

201. Na mwishapo kuzitimiza ibada zenu (za Haji), basi Mkumbukeni Allah kama mnavyowakumbuka baba zenu au kumbukeni zaidi; na kuna baadhi ya watu wanaosema: Mola wetu, Utupe katika dunia; naye katika Akhera hana sehemu.

وَمِنْهُمْ مَّنْ يَّقُوْلُ رَبَّنَآ اٰتِنَا فِى الدُّنْيَا
حَسَنَةً وَّ فِى الْاٰخِرَةِ حَسَنَةً وَّ قِنَا
عَذَابَ النَّارِ ﴿۲۰۱﴾

202. Na miongoni mwao wako wasemao: Mola wetu, Utupe wema duniani na wema katika Akhera, na utulinde na adhabu ya Moto

اُولٰٓئِكَ لَهُمْ نَصِيْبٌ مِّمَّا كَسَبُوْا ؕ وَاللّٰهُ
سَرِيْعُ الْحِسَابِ ﴿۲۰۲﴾

203. Hao ndio watapata sehemu kwa sababu ya yale waliyoyachuma: na Allah ni mwepesi wa kuhesabu.

وَاذْكُرُوا اللّٰهَ فِىْٓ اَيَّامٍ مَّعْدُوْدٰتٍ ؕ فَمَنْ
تَعَجَّلَ فِىْ يَوْمَيْنِ فَلَآ اِثْمَ عَلَيْهِ ۚ وَمَنْ
تَاَخَّرَ فَلَآ اِثْمَ عَلَيْهِ ۙ لِمَنِ اتَّقٰى ؕ وَاتَّقُوا
اللّٰهَ وَاعْلَمُوْٓا اَنَّكُمْ اِلَيْهِ تُحْشَرُوْنَ ﴿۲۰۳﴾

204. Na mkumbukeni Allah katika siku maalumu; lakini afanyaye haraka katika siku mbili, basi si dhambi juu yake; na mwenye kukawia pia si dhambi juu yake, kwa mwenye kumcha Mungu. Na Mcheni Allah, na jueni ya kwamba ninyi mtakusanywa kwake.

Aya 199. *Kuitafuta fadhili.* Waendao kuhiji wameruhusiwa kufanya biashara huko kwa sharti wasijishughulishe kwa kiasi cha kuwasahaulisha kusudi la kufika kwao huko.

Mash'aril Haraam. Neno hili ni jina la kilima kidogo kilichoko Muzdalifa, katikati ya Makka na 'Arafaat. Mahali hapo Mtume s.a.w. aliomba sana kwa Allah.

وَمِنَ النَّاسِ مَنْ يُّعْجِبُكَ قَوْلُهٗ فِي الْحَيٰوةِ الدُّنْيَا وَيُشْهِدُ اللّٰهَ عَلٰى مَا فِيْ قَلْبِهٖ ۙ وَهُوَ اَلَدُّ الْخِصَامِ ﴿٢٠٥﴾

205. Na katika watu yuko ambaye kauli yake juu ya maisha ya dunia inakustaajabisha, naye humshuhudisha Allah kwa yaliyomo moyoni mwake, na hali yeye ni mgomvi mkubwa kabisa.

وَاِذَا تَوَلّٰى سَعٰى فِي الْاَرْضِ لِيُفْسِدَ فِيْهَا وَيُهْلِكَ الْحَرْثَ وَالنَّسْلَ ؕ وَاللّٰهُ لَا يُحِبُّ الْفَسَادَ ﴿٢٠٦﴾

206. Na anapotawala, anakimbia katika ardhi kufanya uharibifu humo, na kuangamiza mimea na watu; na Allah Hapendi uharibifu.

وَاِذَا قِيْلَ لَهُ اتَّقِ اللّٰهَ اَخَذَتْهُ الْعِزَّةُ بِالْاِثْمِ فَحَسْبُهٗ جَهَنَّمُ ؕ وَلَبِئْسَ الْمِهَادُ ﴿٢٠٧﴾

207. Na anapoambiwa, Mche Allah, heshima yake humhimiza afanye dhambi; basi Jahanamu ndilo toshelezo lake, napo hakika ni mahali pabaya pa kupumzikia.

وَمِنَ النَّاسِ مَنْ يَّشْرِيْ نَفْسَهُ ابْتِغَآءَ مَرْضَاتِ اللّٰهِ ؕ وَاللّٰهُ رَءُوْفٌۢ بِالْعِبَادِ ﴿٢٠٨﴾

208. Na yuko miongoni mwa watu auzaye nafsi yake kwa kutaka radhi ya Allah; na Allah ni Mpole kwa watumishi.

يٰۤاَيُّهَا الَّذِيْنَ اٰمَنُوا ادْخُلُوْا فِي السِّلْمِ كَآفَّةً ۪ وَلَا تَتَّبِعُوْا خُطُوٰتِ الشَّيْطٰنِ ؕ اِنَّهٗ لَكُمْ عَدُوٌّ مُّبِيْنٌ ﴿٢٠٩﴾

209. Enyi mlioamini, ingieni nyote katika utii, wala msifuate nyayo za Shetani; bila shaka yeye kwenu ni adui dhahiri.

فَاِنْ زَلَلْتُمْ مِّنْۢ بَعْدِ مَا جَآءَتْكُمُ الْبَيِّنٰتُ فَاعْلَمُوْۤا اَنَّ اللّٰهَ عَزِيْزٌ حَكِيْمٌ ﴿٢١٠﴾

210. Na kama mkiteleza baada ya kuwafikieni Ishara zilizo wazi, basi jueni ya kwanba Allah ni Mwenye nguvu, Mwenye hekima.

هَلْ يَنْظُرُوْنَ اِلَّاۤ اَنْ يَّاْتِيَهُمُ اللّٰهُ فِيْ ظُلَلٍ مِّنَ الْغَمَامِ وَالْمَلٰٓئِكَةُ وَقُضِيَ الْاَمْرُ ؕ وَاِلَى اللّٰهِ تُرْجَعُ الْاُمُوْرُ ﴿٢١١﴾ ع ١٤

211. Hawangojei ila Allah Awafikie katika vivuli vya mawingu na Malaika pia, na shauri likatwe; na mambo yote hurudishwa kwa Allah.

Aya 211. *Mungu Mwenyezi Awafikie katika vivuli vya mawingu.* Hapa zimeelezwa habari za wanafiki na makafiri ya kwamba kwa kuuacha Uislamu, wao hawangoji ila adhabu ya Allah. Tena Allah anawadhihirishia kwa ishara ya kuwa adhabu ya kwanza itawafika katika sura ya mawingu ya mvua, na habari hii ikatimia katika vita vya Badri; mvua ilipopiga, upande wa makafiri uliokuwa mgumu, ukawa matope, na upande wa Waislamu uliokuwa na mchanga, ukawa mgumu. Hivyo makafiri wakatelezateleza na wasiweze kupigana vyema, ikawa ni moja katika sababu zilizowafanya washindwe.

FUNGU 26

سَلْ بَنِيٓ اِسْرَآءِيْلَ كَمْ اٰتَيْنٰهُمْ مِّنْ اٰيَةٍۭ
بَيِّنَةٍ ؕ وَمَنْ يُّبَدِّلْ نِعْمَةَ اللّٰهِ مِنْۢ بَعْدِ
مَا جَآءَتْهُ فَاِنَّ اللّٰهَ شَدِيْدُ الْعِقَابِ ﴿٢١١﴾

212. Waulize wana wa Israeli. Ishara ngapi zilizo wazi Tuliwapa! Na anayezibadilisha neema za Allah baada ya kumfikia, basi hakika Allah ni Mkali wa kuadhibu.

زُيِّنَ لِلَّذِيْنَ كَفَرُوا الْحَيٰوةُ الدُّنْيَا
وَيَسْخَرُوْنَ مِنَ الَّذِيْنَ اٰمَنُوْا ۘ وَالَّذِيْنَ
اتَّقَوْا فَوْقَهُمْ يَوْمَ الْقِيٰمَةِ ؕ وَاللّٰهُ يَرْزُقُ
مَنْ يَّشَآءُ بِغَيْرِ حِسَابٍ ﴿٢١٢﴾

213. Maisha ya dunia yamepambiwa wanaokufuru; na wanawafanyia mzaha waaminio. Na wale wamchao watakuwa juu yao siku ya Kiyama; na Allah Humruzuku Amtakaye bila hesabu.

كَانَ النَّاسُ اُمَّةً وَّاحِدَةً ۟ فَبَعَثَ اللّٰهُ
النَّبِيّٖنَ مُبَشِّرِيْنَ وَمُنْذِرِيْنَ ۪ وَاَنْزَلَ
مَعَهُمُ الْكِتٰبَ بِالْحَقِّ لِيَحْكُمَ بَيْنَ النَّاسِ
فِيْمَا اخْتَلَفُوْا فِيْهِ ؕ وَمَا اخْتَلَفَ فِيْهِ اِلَّا
الَّذِيْنَ اُوْتُوْهُ مِنْۢ بَعْدِ مَا جَآءَتْهُمُ
الْبَيِّنٰتُ بَغْيًۢا بَيْنَهُمْ ۚ فَهَدَى اللّٰهُ الَّذِيْنَ
اٰمَنُوْا لِمَا اخْتَلَفُوْا فِيْهِ مِنَ الْحَقِّ بِاِذْنِهٖ ؕ
وَاللّٰهُ يَهْدِيْ مَنْ يَّشَآءُ اِلٰى صِرَاطٍ
مُّسْتَقِيْمٍ ﴿٢١٣﴾

214. Watu walikuwa kundi moja, basi Allah Akawainua Manabii watoao habari njema na waonyao; na pamoja nao Akateremsha Kitabu kwa haki ili Ahukumu baina ya watu katika yale waliyohitilafiana; na hawakuhitilafiana kwacho ila wale waliokipewa baada ya kuwafikia Ishara zilizo wazi, kwa sababu ya uasi (uliokuwa) kati yao; ndipo Allah Akawaongoza walioamini kwa yale waliyohitilafiana katika haki kwa idhini Yake. Na Allah Humuongoza Amtakaye kwenye njia iliyonyooka.

Aya 214. *Watu wote walikuwa kundi moja.* Mwanzoni wanadamu walikuwa katika hali ya umoja, lakini idadi yao ilipozidi na fikara zao zilipoongezeka wakaanza kuhitilafiana. Hapo Allah akawaleta Manabii katika nchi mbalimbali na katika mataifa mbalimbali ili kuwaongoza katika njia iliyonyooka. Baadaye watu wabaya wakaufanya ule mwongozo walioletewa uwe sababu ya kuzidisha hitilafu zao, basi ndipo Allah Akamtuma Mtume Muhammad *s.a.w.* pamoja na Kitabu cha mwisho, na dini iliyo kamili ili awafundishe watu wote wa ulimwengu, na kwa njia hii dunia iliyoanza kuwa moja ikatakiwa iishi juu ya umoja.

215. Je, mnadhani kwamba mtaingia Peponi na hali hamjafikiwa na mfano wa wale waliopita kabla yenu? Yaliwashika mashaka na dhara na kutetemeshwa sana hata Mtume na walioamini pamoja naye wakasema: Msaada wa Allah utafika lini? Sikilizeni! bila shaka msaada wa Allah uko karibu.

اَمْ حَسِبْتُمْ اَنْ تَدْخُلُوا الْجَنَّةَ وَلَمَّا
يَاْتِكُمْ مَّثَلُ الَّذِيْنَ خَلَوْا مِنْ قَبْلِكُمْ ؕ
مَسَّتْهُمُ الْبَاْسَآءُ وَ الضَّرَّآءُ وَ زُلْزِلُوْا
حَتّٰى يَقُوْلَ الرَّسُوْلُ وَالَّذِيْنَ اٰمَنُوْا مَعَهٗ
مَتٰى نَصْرُ اللّٰهِ ؕ اَلَآ اِنَّ نَصْرَ اللّٰهِ
قَرِيْبٌ ﴿٢١٥﴾

216. Wanakuuliza watoe nini. Sema: Mali yo yote mtakayotoa, basi ni kwa ajili ya wazazi na ndugu na mayatima na maskini na msafiri; na wema wo wote mnaoufanya, basi kwa yakini Allah Anaujua.

يَسْـَٔلُوْنَكَ مَاذَا يُنْفِقُوْنَ ۬ؕ قُلْ مَآ اَنْفَقْتُمْ
مِّنْ خَيْرٍ فَلِلْوَالِدَيْنِ وَالْاَقْرَبِيْنَ
وَالْيَتٰمٰى وَالْمَسٰكِيْنِ وَابْنِ السَّبِيْلِ ؕ وَمَا
تَفْعَلُوْا مِنْ خَيْرٍ فَاِنَّ اللّٰهَ بِهٖ عَلِيْمٌ ﴿٢١٦﴾

Aya 215. *Msaada wa Allah utafika lini?* Maneno haya ni njia moja ya ajabu ya kuomba msaada wa Allah. Hivyo Mungu alipokea maombi yao kwa haraka na kuwajibu, *Sikilizeni! bila shaka msaada wa Allah uko karibu.*

Aya 216. *Khair,* "Mali" Masahaba wa Mtume *s.a.w.* waliposikia kuwa wao hawawezi kufanikiwa mpaka wapite katika njia za taabu na sadaka, kama vile watu wa zamani, mara wakauliza watoe nini. Allah akawajibu, mtatoa *khair,* yaani mali nzuri kwa wingi (Mufradat na Akrab).

Mayatima. Taifa lisiloangalia mayatima wake haliwezi kushinda katika mashindano ya maendeleo. Mayatima wanatakiwa watunzwe vizuri na wakuzwe. Uislamu umeweka sheria zifaazo juu ya kuwatunza mayatima. Hutakiwa mlinzi wa kumtunza yatima na mali yake, achaguliwe; na nduguye ndiye ana haki zaidi ya kuwa mlinzi wake. Mlinzi aangalie mali ya yatima na aiweke mahala pa peke yake. Mlinzi akiwa maskini anaweza kupewa matumizi katika mali hiyo, lakini akiwa hana dhiki hana haki ya kupokea cho chote. Mlinzi ampeleke mtoto kupata elimu au kwenye kazi na uchumi ulio sawa na uwezo na hali yake. Mtoto aangaliwe sana desturi zake na tabia zake, asiachwe kutenda maovu kama apendavyo, wala asitendewe kwa ukali sana hata ikabidi zinyamae bidii za moyo wake hata awe asiyefaa kwa kazi ya namna yo yote. Atendewe kwa wema na upendo maana hana wazazi wa kumhurumia. Yatima akikua na kupata akili itakuwa ni juu ya serikali kuhakikisha busara yake na fahamu yake. Yatima anayeonekana ana uwezo kuangalia shughuli zake mwenyewe basi atatoka ndani ya ulinzi na atapewa mali yake yote yeye mwenyewe. Pia tazama sura 2:221.

217. Mmelazimishwa kupigana vita ingawa mwaichukia; na huenda mchukie kitu nacho ni heri kwenu, na huenda mpende kitu nacho ni shari kwenu. Na Allah Anajua, lakini ninyi hamjui.

كُتِبَ عَلَيْكُمُ الْقِتَالُ وَهُوَ كُرْهٌ لَّكُمْ ۚ
وَعَسٰٓى اَنْ تَكْرَهُوْا شَيْـًٔا وَّهُوَ خَيْرٌ
لَّكُمْ ۚ وَعَسٰٓى اَنْ تُحِبُّوْا شَيْـًٔا وَّهُوَ شَرٌّ
لَّكُمْ ؕ وَاللّٰهُ يَعْلَمُ وَاَنْتُمْ لَا تَعْلَمُوْنَ ﴿٢١٦﴾ ع ٢٦

FUNGU 27

218. Wanakuuliza juu ya kupigana vita katika miezi mitakatifu. Sema: Kupigana vita katika hiyo ni (dhambi) kubwa: na kuwazuilia (watu) njia ya Allah na kumkataa Yeye na Msikiti Mtakatifu, na kuwatoa humo watu waliomo ni (dhambi) kubwa zaidi mbele ya Allah. Na fitina ni mbaya zaidi kuliko kuua. Wala hawataacha kupigana nanyi mpaka wawatoeni katika dini yenu kama wakiweza; na miongoni mwenu atakayetoka katika dini yake, kisha akafa hali yu kafiri, basi hao ndio ambao vitendo vyao vimeharibika katika dunia na Akhera, nao ndio watu wa Motoni, humo watakaa.

يَسْـَٔلُوْنَكَ عَنِ الشَّهْرِ الْحَرَامِ قِتَالٍ فِيْهِ ؕ
قُلْ قِتَالٌ فِيْهِ كَبِيْرٌ ؕ وَصَدٌّ عَنْ سَبِيْلِ
اللّٰهِ وَكُفْرٌۢ بِهٖ وَالْمَسْجِدِ الْحَرَامِ ۗ وَاِخْرَاجُ
اَهْلِهٖ مِنْهُ اَكْبَرُ عِنْدَ اللّٰهِ ۚ وَالْفِتْنَةُ
اَكْبَرُ مِنَ الْقَتْلِ ؕ وَلَا يَزَالُوْنَ
يُقَاتِلُوْنَكُمْ حَتّٰى يَرُدُّوْكُمْ عَنْ دِيْنِكُمْ
اِنِ اسْتَطَاعُوْا ؕ وَمَنْ يَّرْتَدِدْ مِنْكُمْ عَنْ
دِيْنِهٖ فَيَمُتْ وَهُوَ كَافِرٌ فَاُولٰٓئِكَ حَبِطَتْ
اَعْمَالُهُمْ فِى الدُّنْيَا وَالْاٰخِرَةِ ۚ وَاُولٰٓئِكَ
اَصْحٰبُ النَّارِ ۚ هُمْ فِيْهَا خٰلِدُوْنَ ﴿٢١٧﴾

219. Hakika wale walioamini na waliohama na kufanya juhudi katika njia ya Allah - hao ndio wanaotumai rehema za Allah; na Allah ni Msamehevu, Mrehemevu.

اِنَّ الَّذِيْنَ اٰمَنُوْا وَالَّذِيْنَ هَاجَرُوْا
وَجٰهَدُوْا فِىْ سَبِيْلِ اللّٰهِ ۙ اُولٰٓئِكَ يَرْجُوْنَ
رَحْمَتَ اللّٰهِ ؕ وَاللّٰهُ غَفُوْرٌ رَّحِيْمٌ ﴿٢١٨﴾

Aya 217. *Ingawa mwaichukia.* Aya hii inaonyesha waziwazi ya kuwa masahaba za Mtume s.a.w. walipigana vita kwa kujilinda na kujitetea tu, au sivyo walikuwa wakichukia kupigana vita.

220. Wanakuuliza juu ya ulevi na kamari. Sema: Katika hivyo mna dhambi kuu na manufaa kwa watu pia, lakini dhambi yao(hasara) ni kubwa zaidi kuliko manufaa yao. Na wanakuuliza watoe nini. Sema: Vilivyo vizuri. Hivi ndivyo Allah Anavyowabainishieni Aya ili mpate kutafakari.

يَسْـَٔلُوْنَكَ عَنِ الْخَمْرِ وَالْمَيْسِرِ ۭ قُلْ
فِيْهِمَآ اِثْمٌ كَبِيْرٌ وَّمَنَافِعُ لِلنَّاسِ ۡ
وَاِثْمُهُمَآ اَكْبَرُ مِنْ نَّفْعِهِمَا ۭ
وَيَسْـَٔلُوْنَكَ مَاذَا يُنْفِقُوْنَ ۬ ۭ قُلِ الْعَفْوَ ۭ
كَذٰلِكَ يُبَيِّنُ اللّٰهُ لَكُمُ الْاٰيٰتِ لَعَلَّكُمْ
تَتَفَكَّرُوْنَ ۙ﴿۲۱۹﴾

Aya 220. *Ulevi na kamari.* Katika Aya zinazotangulia amri ya kupigana vita imeteremshwa. Kupigana vita kunachukua gharama kubwa mno, hata dola zenye hazina zinazojaa fedha na dhahabu zinahitaji kukopa pauni maelfu-elfu ili kutimiza mahitaji ya askari na vinginevyo. Waarabu walikuwa wakikusanya matumizi hayo kwa kucheza kamari. Waislamu walipoamrishwa kupigana walitaka kujua ni njia zipi za kukusanya mali zinazoruhusiwa na Sheria.

Na pia waliuliza habari za pombe, maana watu wengi wanapofikiwa na msiba au taabu fulani wanapenda kunywa pombe ili wasahau taabu zao. Katika Biblia maskini na mtu anayekaribia kufa wameruhusiwa kutumia divai kwa sababu hii (Mifano ya Maneno 31:4-7). Katika siku za vita askari hunyweshwa pombe nyingi wapate ujasiri wa moyo na wasisikie maumivu. Waarabu walinywesha hata farasi zao pombe. Basi, Waislamu walihitaji kujulishwa, je, vita zao zitakuwa kama za watu wengine au vipi?

Wakati Waislamu walihitaji sana ufunuo utoke mbinguni Allah aliteremsha Aya hizi ambazo zilileta maagizo ya namna ya pekee katika dunia nzima.

INJILI HAIKATAZI VILEO

Katika dini zote, ni dini ya Kiislamu tu inayoharimisha kabisa ulevi na kamari. Mabanyani wanatumia pombe katika baadhi ya ibada zao. Wakristo wanatumia pombe kanisani wakisema ati ni damu ya "Mungu Mwana." Yameandikwa katika Injili ya Yohana 2:7-9, ya kwamba mwujiza wa kwanza wa Yesu ulikuwa ni kugeuza maji yawe "divai njema." Tena hakutengeneza kiasi, bali ilikuwa pombe ya kujaza mabalasi sita. Injili ya Katoliki katika Kiswahili inasema ya kwamba kwa kufanya vile Yesu alionyesha "kwamba hakuna dhambi katika kunywa divai. Dhambi ipo katika ulevi." (uk. 232, maelezo chini ya aya 11)

MAAGIZO YA MTUME.

Mtume *s.a.w.* alisema waziwazi ya kwamba vileo vya kila namna ni haramu (Bukhari), kidogo au kingi (Kashf-ul-Ghummah). Basi Waislamu wanaoshindwa na tabia zao mbaya na kusema kulewa tu ndio kumekatazwa, la si kunywa pombe, basi wajue ya kuwa wanamwasi Allah na Mtume Wake kwa hoja za namna ile. Mtume *s.a.w.* alisema; "Mwislamu anapokunywa pombe imani inamtoka" (Bukhari). Mtume s.a.w. aliharimisha biashara ya pombe (Kashf-ul-Ghummah). Mtu akiruhusiwa kuiba vitu vidogo vidogo pole pole atakuwa mnyang'anyi mkubwa. Tumeona hali ya Wakristo jinsi walivyoteleza miguu kwa huku "kutumia kiasi." Nasi hatuna budi kujihadhari kabisa na vileo.

MASAHABA WANAMTII MTUME

Amri ya kuharimisha divai iliteremka mwisho wa mwaka wa tatu baada ya Hijra au mwanzo wa mwaka wa nne (Zurqaani). Kabla ya kuharimishwa pombe, baadhi ya Waislamu walikuwa wanaitumia. Amri hii iliposhuka, Mtume s.a.w. alituma mtu kunadi masokoni. Saa ile ile baadhi

ya Waislamu walikuwa wakinywa katika nyumba moja na Anas ndiye aliyekuwa akiwanywesha. Mmoja wa wanywaji, Abu Talha alimtuma Anas aende kusikiliza mtangazaji anasemaje. Anas akarudi akamwambia, mtu huyo ametumwa na Mtume s.a.w naye anasema pombe imeharimishwa. Mara Abu Talha akamwamuru Anas kuvunja ule mtungi wa pombe na wote wakaacha (Bukhari).

Inasimuliwa ya kwamba Waislamu wote waliacha kunywa ulevi kwa kusikia sauti ya mnadi tu, wala hakuna hata mmoja aliyemwendea Mtume s.a.w. kuhakikisha kama ni kweli amri hiyo imetoka kwa Allah, ama mtangazaji amewadanganya tu.

Siku hiyo Waislamu walivunja mitungi ya pombe na viriba vilichanwa hata pombe ikaenea katika vijia vya Madina kama maji ya mvua. Jambo hili pia linaonyesha upendo wa dini na moyo wa kutii amri za Allah waliokuwa nao Waislamu wa kwanza.

POMBE ILISHINDA SERIKALI

Serikali ya Amerika ilipitisha amri ya kukataza kabisa ulevi. Lakini watu walioupendelea wakaendelea nao kisirisiri, na wakashughulika nao sana hata serikali, ikashurutishwa kugeuza kanuni yake. Kazi iliyoshindwa kufanya serikali yenye nguvu ya Amerika katika siku hizi za "mwanga na ustaarabu," Mtume s.a.w. aliifanya kwa sauti moja tu katika zama za "giza na ujahili".

Dhambi yao ni kubwa zaidi kuliko manufaa yao. Qur'an Tukufu haisemi kwamba ulevi na kamari ni vitu visivyo na faida asilan. Lakini inatufunza tusiwe wenye kuchukua kitu ambacho dhara yake ni kubwa kuliko faida yake.

Watu wenye fikira nzuri wameanza kutambua dhara iliyoko katika kuandamana na ulevi na kamari. Pombe ni mbegu ya maovu ya namna nyingi. Na kamari ni njia isiyo halali ya kuchuma mali ambayo inaleta chuki, ugomvi, uuaji na umaskini.

Mapadre wengi walitangaza majuzi ya kwamba kucheza kamari ni dhambi. Rais wa Kenya African Union Bwana Jomo Kenyatta, alihimiza Waafrika wasitumie pombe. Si kwamba Biblia inakataza kucheza kamari au Bwana Kenyatta amewakataza wenzake kutumia 'Beer' kwa kufuata amri ya Allah, bali wote hao wameona dhahiri ya kuwa upungufu wa mali na mambo mengi mabaya hufuatana na ulevi na kamari, navyo vinaweza kurudisha nyuma maendeleo ya taifa zima hata katika mambo ya kidunia pia.

Hapa chini tunanukuu kidogo katika maneno mengi yaliyoandikwa na wasio Waislamu wakidhihirisha hatari za pombe na kamari:-

HATARI ZA POMBE

"Ulevi ndilo jambo kubwa katika kuleta magonjwa; na katika magonjwa yote walevi ni wagonjwa wabaya. Katika magonjwa yanayoshika watu wengi vifo katika walevi ni vingi mno, na nguvu yao ya kustahamili magonjwa, majeraha na kazi ngumu hupungua . . . . Ulevi unapunguza maisha. Kampuni za bima ya uhai zimegundua ya kwamba uhai unaotazamiwa wa watu wasiokunywa ulevi ni karibu mara mbili ya ule wa watu wanaolewa. . . . Ulevi na uhalifu wa sheria ni masahibu maarufu, na toka 25 hadi 85 ya kila mia moja wahalifu ni walevi. . . .

"Dhara ya kunywa pombe huonekana katika watoto wa mlevi. . . . Kifafa, wehu, upumbavu, na namna kadha wa kadha za ubovu wa miili, akili, na tabia huonekana katika watoto wa watu wanaokunywa pombe" (Jewish Encyclopaedia i, 333-334; pia tazama Encyclopaedia Britannica 14th Edition, 540; na Encyclopaedia of Religions and Ethics i, 299-301).

HATARI ZA KAMARI

"Uovu wa kucheza kamari bado haujakataliwa. Lord Beaconsfield alisema; 'Kamari ni limashine likubwa linaloharibu tabia za taifa. . . . . Katika miaka 12 (toka 1895-6 mpaka 1906-7) watu katika Uingereza waliojiua wenyewe kwa ajili ya kamari na waliojaribu kujiua, jumla yao walikuwa 156, na kesi za wizi kwa sababu ya kamari zilikuwa 719 na kufilisika 442. Kwa sababu ya mambo haya siyo ajabu kuona ya kwamba katika nchi zote zilizostaarabika kamari imetiliwa vizuizi vya sheria. . .

فِي الدُّنْيَا وَالْاٰخِرَةِ ؕ وَيَسْـَٔلُوْنَكَ عَنِ
الْيَتٰمٰى ؕ قُلْ اِصْلَاحٌ لَّهُمْ خَيْرٌ ؕ وَاِنْ
تُخَالِطُوْهُمْ فَاِخْوَانُكُمْ ؕ وَاللّٰهُ يَعْلَمُ
الْمُفْسِدَ مِنَ الْمُصْلِحِ ؕ وَلَوْ شَآءَ اللّٰهُ
لَاَعْنَتَكُمْ ؕ اِنَّ اللّٰهَ عَزِيْزٌ حَكِيْمٌ ﴿٢٢٠﴾
وَلَا تَنْكِحُوا الْمُشْرِكٰتِ حَتّٰى يُؤْمِنَّ ؕ
وَلَاَمَةٌ مُّؤْمِنَةٌ خَيْرٌ مِّنْ مُّشْرِكَةٍ وَّلَوْ
اَعْجَبَتْكُمْ ۚ وَلَا تُنْكِحُوا الْمُشْرِكِيْنَ حَتّٰى
يُؤْمِنُوْا ؕ وَلَعَبْدٌ مُّؤْمِنٌ خَيْرٌ مِّنْ مُّشْرِكٍ
وَّلَوْ اَعْجَبَكُمْ ؕ اُولٰٓئِكَ يَدْعُوْنَ اِلَى
النَّارِ ۖۚ وَاللّٰهُ يَدْعُوْٓا اِلَى الْجَنَّةِ
وَالْمَغْفِرَةِ بِاِذْنِهٖ ۚ وَيُبَيِّنُ اٰيٰتِهٖ لِلنَّاسِ
لَعَلَّهُمْ يَتَذَكَّرُوْنَ ﴿٢٢١﴾ ع ٢٧ ١١

221. Katika dunia na Akhera. Na wanakuuliza juu ya mayatima. Sema: Kuwatendea mema ndio vizuri, na kama mkichanganyika nao, basi ni ndugu zenu; na Allah Anamjua mfisadi na mtenda mema; na Angalipenda Allah angaliwapeni udhia; hakika Allah ni Mwenye nguvu Mwenye hekima.

222. Wala msiwaoe wanawake washirikina mpaka waamini. Na bila shaka mjakazi mwenye kuamini ni bora kuliko mwanamke mshirikina ingawa awapendezeni. Wala msiwaoze wanaume washirikina mpaka waamini. Na kwa yakini mtumwa mwenye kuamini ni bora kuliko mwanamume mshirikina ingawa awapendezeni; hao wanaita kwenye Moto, na Allah Huita kwenye Pepo na samahani kwa amri Yake. Naye Hueleza Aya Zake kwa watu ili wapate kushika nasaha.

Kamari, kama asemavyo Herbert Spencer, ni namna ya tendo linaloleta furaha kwa kumtia mwingine machungu. Furaha ya anayeshinda ni msiba wa anayepoteza. Kwa hiyo, kitendo cha namna hii ni hakika hakifai kwa ajili ya watu; kinakausha huruma, kinatia tabia kavu ya kujipendelea, na hivyo kunaleta kuharibika kwa tabia zote za mtu. Ni desturi ya kishenzi," (Enc. Rel. Eth. vi. 165-166).

Hayo ndiyo maneno ya watu wanaoijua kamari na ulevi barabara na sasa kwa kuona hatari zake, wenye akili wao wameanza kuchoka navyo. Ingewafaidia sana watu kuacha tabia hizi mbovu zinazoangamiza.

Aya 221. *Wanakuuliza juu ya mayatima.* Kuangalia mayatima ni jambo muhimu kabisa kwa ajili ya faida ya watu wote. Islam inawahimiza wafuasi wake kuwalea mayatima kwa njia iliyo nzuri, na kuwatendea kama watu wa nyumbani na waonekane kama ndugu. Pia tazama sura 2:216.

Aya 222. *Wala msiwaoe wanawake washirikina.* Waislamu wamekatazwa kuwaoa wanawake washirikina, na kuwaoza washirikina binti zao, maana kwa kuoana hivyo inaweza kuleta hatari juu yao na juu ya watoto wao, na wanaweza kupotea bure. Allah amekwisha kuwaokoa katika uchafu wa ushirikina, ya nini kujiingiza tena katika taabu zile za zamani.

FUNGU 28

223. Na wanakuuliza juu ya hedhi. Sema: Hiyo ni udhia; basi jitengeni na wanawake katika hedhi, wala msiwaingilie mpaka wametakasika. Na watakapotakasika, basi wafikieni katika pale Alipowaamuruni Allah; hakika Allah Huwapenda wanaotubu na wanaojitakasa.

وَيَسْـَٔلُوْنَكَ عَنِ الْمَحِيْضِ ؕ قُلْ هُوَ اَذًى ۙ فَاعْتَزِلُوا النِّسَآءَ فِى الْمَحِيْضِ ۙ وَلَا تَقْرَبُوْهُنَّ حَتّٰى يَطْهُرْنَ ۚ فَاِذَا تَطَهَّرْنَ فَاْتُوْهُنَّ مِنْ حَيْثُ اَمَرَكُمُ اللّٰهُ ؕ اِنَّ اللّٰهَ يُحِبُّ التَّوَّابِيْنَ وَيُحِبُّ الْمُتَطَهِّرِيْنَ ﴿۲۲۳﴾

224. Wake zenu ni shamba lenu - basi liendeeni shamba lenu wakati mpendapo, na tangulizieni (wema) nafsi zenu; na Mcheni Allah, na jueni ya kwamba bila shaka mtakutana naye; na uwapashe habari njema waaminio.

نِسَآؤُكُمْ حَرْثٌ لَّكُمْ ۠ فَاْتُوْا حَرْثَكُمْ اَنّٰى شِئْتُمْ ۫ وَقَدِّمُوْا لِاَنْفُسِكُمْ ؕ وَاتَّقُوا اللّٰهَ وَاعْلَمُوْٓا اَنَّكُمْ مُّلٰقُوْهُ ؕ وَبَشِّرِ الْمُؤْمِنِيْنَ ﴿۲۲۴﴾

Aya 223. *Juu ya hedhi.* Mtu hana ruhusa kuingiliana na mkewe katika hali ya hedhi, maana jambo hilo linaweza kuwadhuru wote wawili. Baada ya kukatika damu mtu amekuwa na ruhusa ya kuingiliana naye, lakini ni bora angoje mpaka mkewe ameoga.

Neno la Kiarabu *adha* halina maana ya kitu chenye kuleta madhara. Neno adha ni lazima lieleweke katika maana ya ugonjwa na au usumbufu wa muda. Vinginevyo italetea kueleweka kwamba Allah Ameumba kitu ambacho ni chenye kuleta madhara kwa wanawake, fikra ambayo si sahihi.

Aya 224. *Annaa shi'tum, "Wakati mpendapo."* Maneno haya pia yanafasirika, (1) jinsi mpendavyo na (2) mahali mpendapo.

Wake zenu ni shamba lenu. Aya hii ni ushahidi wa ufasaha wa Qur'an kwa kutumia usemi uliotukuka na ulio safi. Jambo ambalo ni mororo kabisa kuelezeka limeelezwa katika usemi wenye staha sana, na hekima yote ya kuoana na kufikiliana imetajwa katika maneno mafupi kabisa. Inasemwa, *Wake zenu ni shamba lenu.* Mwanamke hakika amefanana na shamba linalopandwa mbengu ya kutoa watoto. Mradi wa Aya hiyo ni namna mbili kwa kutegemea maana ya maneno. *Liendeeni shamba lenu.* Ikiwa kuliendea shamba mradi wake ni kuingiliana, basi maneno hayo yatafahamika hivi: (1) umfikie mkeo kwa namna inayomfaa, sawa na uwezo wake na si kwa namna nyingine: na (2) nyote wawili mjaribu kuiweka mioyo yenu katika hali ya usafi wakati wa kufikiliana ili mtoto atayetokana na tendo hilo naye apate usafi huo. Mtume s.a.w. alisema, "Mume anapomwingilia mkewe, wote wawili waombe kwa Allah na waseme. Mola wetu, utuepushe sote wawili na Shetani, na kama ukituruzuku mtoto, basi naye umwepushe na Shetani" (Muslim).

Lakini, kama kuliendea shamba mradi wake ni kuchagua mke au kushughulika naye, maneno haya liendeeni shamba lenu "mpendavyo," yatafahamika hivi; (1) Kwamba uchague mke anayefaa sana kuwa shamba, yaani (a) awe *waluud,* yaani, aweze kuzaa, asiwe tasa; (b) awe mwenye afya nzuri, awezaye kuzaa watoto wenye afya njema; (c) awe na sifa za kutosha kwa kuwapa watoto mafunzo mema na (d) waduud , yaani mwenye tabia ya huba na mapenzi ili makazi ya nyumbani

225. Wala msimfanye Allah shabaha ya viapo vyenu ili msipate kufanya wema na kuogopa na kupatanisha baina ya watu. Na Allah ni Mwenye kusikia, Mwenye kujua.

وَلَا تَجْعَلُوا اللّٰهَ عُرْضَةً لِّاَيْمَانِكُمْ اَنْ تَبَرُّوْا وَتَتَّقُوْا وَتُصْلِحُوْا بَيْنَ النَّاسِ ؕ وَاللّٰهُ سَمِيْعٌ عَلِيْمٌ ﴿۲۲۵﴾

226. Allah Hatawashikeni kwa sababu ya upuuzi katika viapo vyenu, bali Atawashikeni kwa sababu ya yale iliyofanya mioyo yenu; na Allah ndiye Msamehevu, Mpole.

لَا يُؤَاخِذُكُمُ اللّٰهُ بِاللَّغْوِ فِيْٓ اَيْمَانِكُمْ وَلٰكِنْ يُّؤَاخِذُكُمْ بِمَا كَسَبَتْ قُلُوْبُكُمْ ؕ وَاللّٰهُ غَفُوْرٌ حَلِيْمٌ ﴿۲۲۶﴾

227. Kwa wale wanaoapa kwamba watajitenga na wake zao, (muda wao) ni kungoja miezi minne; na kama wakirejea, basi hakika Allah ni Msamehevu, Mrehemevu.

لِلَّذِيْنَ يُؤْلُوْنَ مِنْ نِّسَآئِهِمْ تَرَبُّصُ اَرْبَعَةِ اَشْهُرٍ ۚ فَاِنْ فَآءُوْ فَاِنَّ اللّٰهَ غَفُوْرٌ رَّحِيْمٌ ﴿۲۲۷﴾

228. Na wakiazimia talaka, basi kwa hakika Allah ni Mwenye kusikia, Mwenye kujua.

وَاِنْ عَزَمُوا الطَّلَاقَ فَاِنَّ اللّٰهَ سَمِيْعٌ عَلِيْمٌ ﴿۲۲۸﴾

---

yawe ya kupendana na masikilizano na watoto wafaidike kwayo. (2) Kwamba umtunze mkeo na kumtendea kwa wema ili maisha yake yawe ya furaha na kutosheka, na ili awe mwelekevu kuwalea watoto vizuri. (3) Kwamba nyote wawili mjiweke kwenye hali ya afya njema na mwenendo wa ucha-Mungu ili mbegu ya shamba lenu pia iwe yenye nguvu katika hali zote.

Aya 226. *Upuuzi katika viapo*. Mtu akila yamini pasipo kukusudia, yamini ya namna hiyo huitwa *laghwu,* kama vile watu wengi walivyo na mazoea ya kuapaapa au kuapa wakati wa hasira. Ingawa viapo vya namna hii kwa mujibu wa kanuni ya Sharia na kanuni ya serikali si kitu, lakini watu wa namna hii wanaitwa wapuuzi, na wanaweza kuonja taabu za upuuzi wao.

Aya 227. *Iilaa,* ni tendo la mtu anapoapa kuwa hatokaribiana na mkewe. Katika hali ya *Iilaa* mume hawezi Kumwacha mkewe kwa muda wa zaidi ya miezi minne. Kama hakumchukua mke wake katika muda huo, basi ikipita miezi minne itakuwa ni talaka.

Aya 228. *Wakiazimia talaka.* Kwa mujibu wa sheria ya Kiislamu mume anayo haki ya kumwacha mkewe akiona ameshurutishwa na haja fulani iliyo halali. Katika dini ya Kikristo pia mtu anaweza kumwacha mkewe, lakini kwa sharti moja tu la uasherati (Matt. 5:32). Dini ya Islam inasema, si mambo ya uasherati tu yanayoweza kumchukiza mtu katika habari za mkewe, bali yanaweza kupatikana mambo mengine pia. Basi kwa ajili hii haikuelezwa sababu ya talaka iliyo maalumu. Ubovu wa kanuni ya Kikristo umekuwa wazi sana katika nchi zote za Wakristo. Lakini juu ya hayo Wakristo, hasa mapadre wanaendelea kuleta upinzani wao usio na dalili juu ya kanuni ya Kiislamu ya talaka. Jambo hili linaonyesha kuwa mapadre wanapinza kwa shauri ya

وَالْمُطَلَّقٰتُ يَتَرَبَّصْنَ بِاَنْفُسِهِنَّ ثَلٰثَةَ
قُرُوْٓءٍ ؕ وَلَا يَحِلُّ لَهُنَّ اَنْ يَّكْتُمْنَ مَا
خَلَقَ اللّٰهُ فِيْٓ اَرْحَامِهِنَّ اِنْ كُنَّ يُؤْمِنَّ
بِاللّٰهِ وَالْيَوْمِ الْاٰخِرِ ؕ وَبُعُوْلَتُهُنَّ اَحَقُّ
بِرَدِّهِنَّ فِيْ ذٰلِكَ اِنْ اَرَادُوْٓا اِصْلَاحًا ؕ
وَلَهُنَّ مِثْلُ الَّذِيْ عَلَيْهِنَّ بِالْمَعْرُوْفِ ۠
وَلِلرِّجَالِ عَلَيْهِنَّ دَرَجَةٌ ؕ وَاللّٰهُ عَزِيْزٌ
حَكِيْمٌ ﴿٢٢٨﴾ ع

229. Na wanawake waliopewa talaka wangoje mpaka hedhi tatu, wala haiwapasi kuficha Aliyoumba Allah katika matumbo yao, ikiwa wanamwamini Allah na siku ya Mwisho; na waume wao wana haki zaidi ya kuwarejesha katika muda huo, kama wakitaka isilahi. Nao (wanawake) wanayo haki sawa na ile iliyo juu yao kwa sheria; na wanaume wana daraja moja zaidi kuliko wao, na Allah ni Mwenye nguvu, Mwenye hekima

FUNGU 29

اَلطَّلَاقُ مَرَّتٰنِ ۪ فَاِمْسَاكٌۢ بِمَعْرُوْفٍ اَوْ
تَسْرِيْحٌۢ بِاِحْسَانٍ ؕ وَلَا يَحِلُّ لَكُمْ اَنْ
تَاْخُذُوْا مِمَّآ اٰتَيْتُمُوْهُنَّ شَيْـًٔا اِلَّآ اَنْ
يَّخَافَآ اَلَّا يُقِيْمَا حُدُوْدَ اللّٰهِ ؕ فَاِنْ
خِفْتُمْ اَلَّا يُقِيْمَا حُدُوْدَ اللّٰهِ ۙ فَلَا جُنَاحَ
عَلَيْهِمَا فِيْمَا افْتَدَتْ بِهٖ ؕ تِلْكَ حُدُوْدُ اللّٰهِ
فَلَا تَعْتَدُوْهَا ۚ وَمَنْ يَّتَعَدَّ حُدُوْدَ اللّٰهِ
فَاُولٰٓئِكَ هُمُ الظّٰلِمُوْنَ ﴿٢٢٩﴾

230. Talaka (hutolewa) mara mbili; kisha ni kuwaweka kwa wema au kuwaacha kwa ihsani; wala si halali kwenu kuchukua cho chote mlichowapa (wake zenu), isipokuwa wote wawili wakiogopa ya kwamba hawataweza kusimamisha mipaka ya Allah; na kama mkiogopa kwamba hawataweza kusimamisha mipaka ya Allah, basi si aibu kwao kupokea ajikomboleacho mwanamke. Hii ndiyo mipaka ya Allah, basi msiiruke. Na atakayeiruka mipaka ya Allah, basi hao ndio wadhalimu.

husuda tu na hakuna kitu kingine. Habari za talaka katika dini ya Kiislamu zimewekewa vizuizi sana. Mtume s.a.w. amesema, "Jambo lililo halali lichukizalo sana mbele ya Allah ni talaka" (Dawud, sura ya *talaaq*). Lakini kama mume na mke baada ya kila juhudi ya mapatano wasiweze kukaa pamoja, wameruhusiwa kuachana. Mume anaambiwa, ukitaka kumwacha mke wako uangalie mambo haya:- (1) Talaka itolewe moja moja baada ya mke kutoka hedhi kabla hajaingiliwa. (2) Mke lazima akae nyumbani kwa mumewe mpaka tohara tatu zipite. (3) Mume anayo hiari ya kumrejesha mke wake kabla haujaisha muda wa tohara tatu. Na kama mke alikuwa hajalipwa mahari yake lazima apewe kabla ya kutoa talaka ya mwisho.

231. Na kama amempa talaka (ya tatu), basi (mwanamke huyo) si halali kwake baada ya hayo mpaka aolewe na mume mwingine; na (mwanamume huyo) akimwacha, basi hapana aibu kwao (mume yule wa kwanza na mwanamke huyo) kurejeana ikiwa kama wana yakini ya kwamba wote wawili watasimamisha mipaka ya Allah. Na hii ni mipaka ya Allah Anayoibainisha kwa watu wajuao.

فَاِنْ طَلَّقَهَا فَلَا تَحِلُّ لَهٗ مِنْۢ بَعْدُ حَتّٰى
تَنْكِحَ زَوْجًا غَيْرَهٗ ؕ فَاِنْ طَلَّقَهَا فَلَا
جُنَاحَ عَلَيْهِمَآ اَنْ يَّتَرَاجَعَآ اِنْ ظَنَّآ اَنْ
يُّقِيْمَا حُدُوْدَ اللّٰهِ ؕ وَتِلْكَ حُدُوْدُ اللّٰهِ
يُبَيِّنُهَا لِقَوْمٍ يَّعْلَمُوْنَ ﴿٢٣١﴾

232. Na mtakapowapa wanawake talaka, nao wakafikia eda yao, basi washikeni kwa wema au waacheni kwa wema, wala msiwaweke kwa kuwapa dhara mkaruke mipaka; na atakayefanya hivyo, hakika yeye amejidhulumu mwenyewe. Wala msizifanyie mzaha aya za Allah; na kumbukeni neema za Allah zilizo juu yenu, na pia Aliyoyateremsha katika Kitabu na hekima Anayowaonyeni kwayo. Na Mcheni Allah na jueni kwamba Allah ni Mjuzi wa kila kitu.

وَاِذَا طَلَّقْتُمُ النِّسَآءَ فَبَلَغْنَ اَجَلَهُنَّ
فَاَمْسِكُوْهُنَّ بِمَعْرُوْفٍ اَوْ سَرِّحُوْهُنَّ
بِمَعْرُوْفٍ ۖ وَلَا تُمْسِكُوْهُنَّ ضِرَارًا
لِّتَعْتَدُوْا ۚ وَمَنْ يَّفْعَلْ ذٰلِكَ فَقَدْ ظَلَمَ
نَفْسَهٗ ؕ وَلَا تَتَّخِذُوْٓا اٰيٰتِ اللّٰهِ هُزُوًا ۫
وَاذْكُرُوْا نِعْمَتَ اللّٰهِ عَلَيْكُمْ وَمَآ اَنْزَلَ
عَلَيْكُمْ مِّنَ الْكِتٰبِ وَالْحِكْمَةِ يَعِظُكُمْ
بِهٖ ؕ وَاتَّقُوا اللّٰهَ وَاعْلَمُوْٓا اَنَّ اللّٰهَ بِكُلِّ
شَيْءٍ عَلِيْمٌ ﴿٢٣٢﴾ ع ٢٩ ٣ ١٣ الثلثة

FUNGU 30

233. Na mtakapowapa wanawake talaka (ya kwanza au ya pili) nao wakamaliza eda yao, basi msiwazuie kuolewa na waume zao endapo baina yao wamepatana kwa wema. Hayo anaonywa nayo yule miongoni mwenu anayemwamini Allah na siku ya Mwisho. Hayo ni mazuri mno kwenu na safi kabisa; na Allah Anajua lakini ninyi hamjui.

وَاِذَا طَلَّقْتُمُ النِّسَآءَ فَبَلَغْنَ اَجَلَهُنَّ فَلَا
تَعْضُلُوْهُنَّ اَنْ يَّنْكِحْنَ اَزْوَاجَهُنَّ اِذَا
تَرَاضَوْا بَيْنَهُمْ بِالْمَعْرُوْفِ ؕ ذٰلِكَ
يُوْعَظُ بِهٖ مَنْ كَانَ مِنْكُمْ يُؤْمِنُ بِاللّٰهِ
وَالْيَوْمِ الْاٰخِرِ ؕ ذٰلِكُمْ اَزْكٰى لَكُمْ
وَاَطْهَرُ ؕ وَاللّٰهُ يَعْلَمُ وَاَنْتُمْ لَا تَعْلَمُوْنَ ﴿٢٣٣﴾

234. Na wanawake waliozaa wawanyonyeshe watoto wao miaka miwili kwa (mwanaume) anayetaka kukamilisha kunyonyesha; na ni juu ya baba yake chakula chao na nguo zao kwa sheria; Nafsi yo yote haikalifishwi ila kwa kadiri ya wasaa wake. Mama asiwekwe taabuni kwa ajili ya mtoto wake, wala baba kwa ajili ya mtoto wake, na juu ya mrithi ni kama hivyo. Na kama wote wawili wakitaka kumwachisha ziwa, kwa kuridhiana na kushauriana, basi si dhambi kwao. Na kama mkitaka kuwapatia watoto wenu mama wa kuwanyonyesha, basi haitakuwa aibu juu yenu kama mkitoa sawa na desturi. Na Mcheni Allah, na jueni kwamba Allah Anayaona mnayoyatenda.

وَالْوَالِدٰتُ يُرْضِعْنَ اَوْلَادَهُنَّ حَوْلَيْنِ
كَامِلَيْنِ لِمَنْ اَرَادَ اَنْ يُّتِمَّ الرَّضَاعَةَ ؕ
وَعَلَى الْمَوْلُوْدِ لَهٗ رِزْقُهُنَّ وَكِسْوَتُهُنَّ
بِالْمَعْرُوْفِ ؕ لَا تُكَلَّفُ نَفْسٌ اِلَّا
وُسْعَهَا ۚ لَا تُضَآرَّ وَالِدَةٌۢ بِوَلَدِهَا وَلَا
مَوْلُوْدٌ لَّهٗ بِوَلَدِهٖ ۘ وَعَلَى الْوَارِثِ مِثْلُ
ذٰلِكَ ۚ فَاِنْ اَرَادَا فِصَالًا عَنْ تَرَاضٍ مِّنْهُمَا
وَتَشَاوُرٍ فَلَا جُنَاحَ عَلَيْهِمَا ؕ وَاِنْ اَرَدْتُّمْ
اَنْ تَسْتَرْضِعُوْٓا اَوْلَادَكُمْ فَلَا جُنَاحَ
عَلَيْكُمْ اِذَا سَلَّمْتُمْ مَّآ اٰتَيْتُمْ
بِالْمَعْرُوْفِ ؕ وَاتَّقُوا اللّٰهَ وَاعْلَمُوْٓا اَنَّ
اللّٰهَ بِمَا تَعْمَلُوْنَ بَصِيْرٌ ﴿٢٣٣﴾

235. Na wale wanaofishwa miongoni mwenu na kuacha nyuma wake, hawa wangoje miezi minne na siku kumi; na wanapofikia muda wao, basi si aibu juu yenu katika yale wanayoyafanya kwa nafsi zao kwa (kufuata) sheria; na Allah Anazo habari za mnayoyatenda.

وَالَّذِيْنَ يُتَوَفَّوْنَ مِنْكُمْ وَيَذَرُوْنَ
اَزْوَاجًا يَّتَرَبَّصْنَ بِاَنْفُسِهِنَّ اَرْبَعَةَ
اَشْهُرٍ وَّعَشْرًا ۚ فَاِذَا بَلَغْنَ اَجَلَهُنَّ فَلَا
جُنَاحَ عَلَيْكُمْ فِيْمَا فَعَلْنَ فِيْٓ اَنْفُسِهِنَّ
بِالْمَعْرُوْفِ ؕ وَاللّٰهُ بِمَا تَعْمَلُوْنَ خَبِيْرٌ ﴿٢٣٤﴾

Aya 234. Mwanamke mwenye mimba akiachwa, na baadaye azae mtoto, nani atachukua madaraka ya kunyonyesha? Allah Anasema. Muda kamili wa kumnyonyesha mtoto ni miaka miwili; lakini kama baba na mama wanapatana kwa muda ulio mdogo kuliko huu pia si vibaya. Matumizi ya mama yatatolewa na baba, ila wote wawili washike uadilifu, mmoja wao asimtaabishe mwenziwe kwa ajili ya mtoto.

Aya 235. Wanawake wanaofiwa na waume zao eda yao ni miezi minne na siku kumi. Ukipita muda huu wanayo hiari ya kuolewa kama Alivyosema Allah ya kuwa wanawake wajane waozwe (sura 24:33).

وَلَا جُنَاحَ عَلَيْكُمْ فِيمَا عَرَّضْتُمْ بِهٖ مِنْ
خِطْبَةِ النِّسَآءِ اَوْ اَكْنَنْتُمْ فِيْٓ اَنْفُسِكُمْ ؕ
عَلِمَ اللّٰهُ اَنَّكُمْ سَتَذْكُرُوْنَهُنَّ وَلٰكِنْ لَّا
تُوَاعِدُوْهُنَّ سِرًّا اِلَّآ اَنْ تَقُوْلُوْا قَوْلًا
مَّعْرُوْفًا ۬ وَلَا تَعْزِمُوْا عُقْدَةَ النِّكَاحِ
حَتّٰى يَبْلُغَ الْكِتٰبُ اَجَلَهٗ ؕ وَاعْلَمُوْٓا اَنَّ
اللّٰهَ يَعْلَمُ مَا فِيْٓ اَنْفُسِكُمْ فَاحْذَرُوْهُ ۚ
وَاعْلَمُوْٓا اَنَّ اللّٰهَ غَفُوْرٌ حَلِيْمٌ ﴿۲۳۵﴾ ع ۱۴ ۲۰

236. Wala si dhambi kwenu katika kupeleka habari ya posa kwa ishara kuwaoa wake (waliofiwa) au mliyoyaficha mioyoni mwenu; Allah Anajua kwamba ninyi karibuni mtawakumbuka; lakini msifunge nao ahadi kwa siri, isipokuwa mseme maneno yaliyo bora; wala msiazimie kufunga ndoa mpaka muda ulioandikwa ufikie mwisho wake. Na jueni ya kwamba Allah Anayajua yaliyomo katika nafsi zenu, basi jihadharini naye. Na jueni kwamba Allah ni Msamehevu, Mvumilivu.

FUNGU 31

لَا جُنَاحَ عَلَيْكُمْ اِنْ طَلَّقْتُمُ النِّسَآءَ مَا
لَمْ تَمَسُّوْهُنَّ اَوْ تَفْرِضُوْا لَهُنَّ فَرِيْضَةً ۖۗ
وَّمَتِّعُوْهُنَّ ۚ عَلَى الْمُوْسِعِ قَدَرُهٗ وَعَلَى
الْمُقْتِرِ قَدَرُهٗ ۚ مَتَاعًۢا بِالْمَعْرُوْفِ ۚ حَقًّا
عَلَى الْمُحْسِنِيْنَ ﴿۲۳۶﴾

237. Si dhambi kwenu kama mkiwapa wanawake talaka ambapo hamjawagusa au kuwawekea mahari. Na wapatieni matumizi - mwenye wasaa kadiri awezavyo, na mwenye dhiki kadiri awezavyo - matumizi kama ilivyo desturi; ndio wajibu kwa wafanyao hisani.

وَاِنْ طَلَّقْتُمُوْهُنَّ مِنْ قَبْلِ اَنْ تَمَسُّوْهُنَّ
وَقَدْ فَرَضْتُمْ لَهُنَّ فَرِيْضَةً فَنِصْفُ مَا
فَرَضْتُمْ اِلَّآ اَنْ يَّعْفُوْنَ اَوْ يَعْفُوَا الَّذِيْ

238. Na kama mkiwapa talaka kabla ya kuwagusa, na mmekwisha wawekea mahari, basi (wapeni) nusu ya mliyoyaweka, isipokuwa wanawake wenyewe waache au yule (mtu)

Aya 236. Kwa mujibu wa Aya hii imekatazwa kufanya mapatano ya ndoa waziwazi na wanawake waliomo katika eda za waume wao waliofariki. Lakini kudokeza habari kwa ishara kwa njia iliyo nzuri haikukatazwa.

Aya 237. Wakati mwingine mtu analazimika kumwacha mkewe kabla ya kumleta nyumbani kwake na kabla ya kukata mahari. Basi wakati wa namna hii ni lazima mume ampe mke wake zawadi kabla ya kuagana naye iliyo sawa na uwezo wake ili hasira na bughudha ipowe moyoni.

Aya 238. Mtu akitaka kumwacha mkewe ambaye hajaingiliana naye, na hali wamekwisha patana mahari, basi katika hali ya namna hii ni wajibu wa mume kumpa mkewe nusu ya mahari.

بِيَدِهٖ عُقْدَةُ النِّكَاحِ ؕ وَاَنْ تَعْفُوْٓا اَقْرَبُ
لِلتَّقْوٰى ؕ وَلَا تَنْسَوُا الْفَضْلَ بَيْنَكُمْ ؕ
اِنَّ اللّٰهَ بِمَا تَعْمَلُوْنَ بَصِيْرٌ ﴿٢٣٧﴾

ambaye kifungo cha ndoa ki mikononi mwake aache (haki yake). Na ya kwamba muache ndiyo karibu sana na utawa. Wala msisahau kufanyiana hisani; hakika Allah Anayaona mnayoyafanya.

حٰفِظُوْا عَلَى الصَّلَوٰتِ وَالصَّلٰوةِ
الْوُسْطٰى ۗ وَقُوْمُوْا لِلّٰهِ قٰنِتِيْنَ ﴿٢٣٨﴾

239. Zingatieni sala, na hasa sala ya katikati, na simameni kwa kumtii Allah.

فَاِنْ خِفْتُمْ فَرِجَالًا اَوْ رُكْبَانًا ۚ فَاِذَآ
اَمِنْتُمْ فَاذْكُرُوا اللّٰهَ كَمَا عَلَّمَكُمْ مَّا لَمْ
تَكُوْنُوْا تَعْلَمُوْنَ ﴿٢٣٩﴾

240. Na kama mkiwa na hofu basi (salini) mkitembea au mkipanda ; na mtakapokuwa katika amani, basi Mkumbukeni Allah kama Alivyowafunzeni yale mliyokuwa hamyajui.

وَالَّذِيْنَ يُتَوَفَّوْنَ مِنْكُمْ وَيَذَرُوْنَ
اَزْوَاجًا ۖ وَّصِيَّةً لِّاَزْوَاجِهِمْ مَّتَاعًا اِلَى
الْحَوْلِ غَيْرَ اِخْرَاجٍ ۚ فَاِنْ خَرَجْنَ فَلَا
جُنَاحَ عَلَيْكُمْ فِيْ مَا فَعَلْنَ فِيْٓ اَنْفُسِهِنَّ
مِنْ مَّعْرُوْفٍ ؕ وَاللّٰهُ عَزِيْزٌ حَكِيْمٌ ﴿٢٤٠﴾

241. Na wale wanaofishwa miongoni mwenu na kubakisha wake, wasia kwa ajili ya wake zao ni kupata matumizi ya mwaka mmoja bila kutolewa; na kama wanawake wenyewe wakiondoka, basi si kosa juu yenu katika yale waliyoyafanya kwa nafsi zao wenyewe sawa na desturi. Na Allah ni Mwenye nguvu, Mwenye hekima.

وَلِلْمُطَلَّقٰتِ مَتَاعٌۢ بِالْمَعْرُوْفِ ؕ حَقًّا
عَلَى الْمُتَّقِيْنَ ﴿٢٤١﴾

242. Na wanawake waliopewa talaka pia wapewe matumizi sawa na desturi; huo ndio wajibu kwa wamchao Allah.

كَذٰلِكَ يُبَيِّنُ اللّٰهُ لَكُمْ اٰيٰتِهٖ لَعَلَّكُمْ
تَعْقِلُوْنَ ﴿٢٤٢﴾ ع ١٥ ٣١

243. Hivyo ndivyo Anavyowabainishieni Allah aya zake ili mpate kufahamu.

Aya 239. *Sala ya katikati.* Wengine wanasema, Sala ya katikati ni Sala ya Alfajiri, ambapo wengine wanafikiri Sala ya katikati ni Sala ya Adhuhuri au ya Alasiri au ya Tahajjud. Lakini kwa hakika Sala ya katikati ni kila Sala inayomkuta mtu katikati ya shughuli zake, maana katika hali ya namna hii mtu anaweza kupitiwa Sala ikamponyoka, hivyo amehimizwa kuangalia Sala ya namna hii.

FUNGU 32

244. Je, hukuwaona wale waliotoka katika majumba yao, nao walikuwa maelfu wakiogopa mauti? Basi Allah Akawaambia; Kufeni; kisha Akawahuisha. Kwa hakika Allah ni Mwenye fadhili juu ya watu, lakini watu wengi hawashukuru.

اَلَمْ تَرَ اِلَى الَّذِيْنَ خَرَجُوْا مِنْ دِيَارِهِمْ
وَهُمْ اُلُوْفٌ حَذَرَ الْمَوْتِ ۪ فَقَالَ لَهُمُ
اللّٰهُ مُوْتُوْا ۫ ثُمَّ اَحْيَاهُمْ ؕ اِنَّ اللّٰهَ لَذُوْ
فَضْلٍ عَلَى النَّاسِ وَلٰكِنَّ اَكْثَرَ النَّاسِ
لَا يَشْكُرُوْنَ ﴿٢٤٣﴾

245. Na piganeni katika njia ya Allah, na jueni kwamba Allah ndiye Asikiaye, Ajuaye.

وَقَاتِلُوْا فِيْ سَبِيْلِ اللّٰهِ وَاعْلَمُوْٓا اَنَّ اللّٰهَ
سَمِيْعٌ عَلِيْمٌ ﴿٢٤٤﴾

246. Ni nani atakayemkatia Allah sehemu bora (ya mali yake) ili Allah Amzidishie uzidisho mwingi, na Allah Hupokea na Huzidisha, na Kwake mtarejeshwa.

مَنْ ذَا الَّذِيْ يُقْرِضُ اللّٰهَ قَرْضًا حَسَنًا
فَيُضٰعِفَهٗ لَهٗٓ اَضْعَافًا كَثِيْرَةً ؕ وَاللّٰهُ
يَقْبِضُ وَيَبْصُۜطُ ۪ وَاِلَيْهِ تُرْجَعُوْنَ ﴿٢٤٥﴾

247. Je, hukuwaona wakubwa wa wana wa Israeli baada ya Musa, walipomwambia Nabii wao: Utuwekee mfalme ili tupigane katika njia ya Allah? Yeye akasema. Je, haielekei ya kuwa hamtapigana ikiwa mtalazimishwa kupigana? Wakasema kimetufika nini mpaka tusipigane vita katika njia ya Allah

اَلَمْ تَرَ اِلَى الْمَلَاِ مِنْۢ بَنِيْٓ اِسْرَآءِيْلَ مِنْۢ
بَعْدِ مُوْسٰى ۘ اِذْ قَالُوْا لِنَبِيٍّ لَّهُمُ ابْعَثْ لَنَا
مَلِكًا نُّقَاتِلْ فِيْ سَبِيْلِ اللّٰهِ ؕ قَالَ هَلْ
عَسَيْتُمْ اِنْ كُتِبَ عَلَيْكُمُ الْقِتَالُ اَلَّا
تُقَاتِلُوْا ؕ قَالُوْا وَمَا لَنَآ اَلَّا نُقَاتِلَ فِيْ

Aya 244. Habari za wana wa Israeli waliokimbia mateso ya Firauni zimeelezwa hapa. Qur'an inaeleza kuwa walikuwa watu elfu chache. Watu hao waliogopa mauti na wakakataa kupigana na kumsaidia Nabii Musa. Basi hapo Allah akawatia katika masumbufu ya jangwani yaliyofanana na mauti, na watu wale wabaya walipokufa na watoto wao wakakua, Allah akawasaidia na akawahuisha uhai wa heshima, na wakaingia katika nchi waliyoahidiwa kupewa.

Aya 246. Watu wo wote wanaotaka kuinuka vizuri ni lazima kwao kutoa mali kwa wingi ili waweze kuendelea vizuri. Hapa Allah Anawahimiza Waislamu watoe mali katika njia ya Mungu. Neno lililotumika hapa linaweza kufasiriwa hivi. "Ni nani atakayemtolea Allah karadhi iliyo nzuri." Basi kwa tafsiri hiyo, Allah anasema mali zenu zitakuwa kama deni kwa Allah na mtarudishiwa malipo yake, yaani mali mtakazozitoa katika njia ya Allah haziwezi kupotea.

سَبِيْلِ اللّٰهِ وَقَدْ اُخْرِجْنَا مِنْ دِيَارِنَا
وَاَبْنَآئِنَا ؕ فَلَمَّا كُتِبَ عَلَيْهِمُ الْقِتَالُ
تَوَلَّوْا اِلَّا قَلِيْلًا مِّنْهُمْ ؕ وَاللّٰهُ عَلِيْمٌۢ
بِالظّٰلِمِيْنَ ﴿۲۴۶﴾

na hali tumetolewa katika nyumba zetu na watoto wetu? Lakini walipoandikiwa kupigana vita, wakageuka isipokuwa wachache miongoni mwao. Na Allah Anawajua sana wadhalimu.

وَقَالَ لَهُمْ نَبِيُّهُمْ اِنَّ اللّٰهَ قَدْ بَعَثَ
لَكُمْ طَالُوْتَ مَلِكًا ؕ قَالُوْٓا اَنّٰى يَكُوْنُ
لَهُ الْمُلْكُ عَلَيْنَا وَنَحْنُ اَحَقُّ بِالْمُلْكِ مِنْهُ
وَلَمْ يُؤْتَ سَعَةً مِّنَ الْمَالِ ؕ قَالَ اِنَّ اللّٰهَ
اصْطَفٰىهُ عَلَيْكُمْ وَزَادَهٗ بَسْطَةً فِي الْعِلْمِ
وَالْجِسْمِ ؕ وَاللّٰهُ يُؤْتِيْ مُلْكَهٗ مَنْ يَّشَآءُ ؕ
وَاللّٰهُ وَاسِعٌ عَلِيْمٌ ﴿۲۴۷﴾

248. Na Nabii wao akawaambia: Hakika Allah Amewatoleeni Taluti kuwa mfalme. Wakasema: Anawezaje kuwa na ufalme juu yetu na hali sisi tumestahili zaidi kupata ufalme kuliko yeye, naye hakupewa wasaa wa mali? Akasema: Bila shaka Allah Amemchagua juu yenu na Amemzidishia wasaa wa elimu na mwili. Na Allah Humpa ufalme wake Amtakaye. Na Allah ni Mwenye wasaa, Mwenye kujua.

وَقَالَ لَهُمْ نَبِيُّهُمْ اِنَّ اٰيَةَ مُلْكِهٖٓ اَنْ
يَّاْتِيَكُمُ التَّابُوْتُ فِيْهِ سَكِيْنَةٌ مِّنْ رَّبِّكُمْ
وَبَقِيَّةٌ مِّمَّا تَرَكَ اٰلُ مُوْسٰى وَاٰلُ هٰرُوْنَ

249. Na Nabii wao akawaambia: Hakika alama ya ufalme wake ni kuwafikieni moyo wenye utulivu ndani yake, utokao kwa Mola wenu, na masazo

---

Aya 248. *Taluti.* Neno hili ni jina la sifa alilopangwa mfalme mmoja wa Kiisraeli, aliyekuwako miaka mia mbili kabla ya Nabii Daudi. Mufasirina wengine wa Qur'an wanaeleza kuwa Saul ndiye aliyepewa jina hilo; lakini kwa hakika habari hizi zinatimia juu ya Gideon (Waamuzi 6-8). Sababu katika wakati wake ndio watu walifukuzwa katika majumba yao, mtu mmoja asiyekuwa mfalme akawekwa kuwa mfalme. Allah akamsaidia huyo mfalme na wafuasi wake kwa kuwapa *Taabuut* (Moyo). Watu wake walijaribiwa kwa maji, nao walikuwa wachache sana mbele ya maadui zao, hata hivyo idadi yao ikapungua kwa sababu ya jaribio hilo. Lakini juu ya hayo walifanikiwa kuwashinda maadui zao.

Wakristo huleta upinzani juu ya maneno hayo, wakisema kuwa habari hizi zilizoelezwa hapa ni za nyakati mbalimbali zilizoachana kwa miaka mia mbili. Majibu yake ni haya kuwa, Qur'an ilikusudia kueleza habari za nyakati hizi mbili pamoja kwa kuwa mataifa mbalimbali ya wana wa Israeli yalianza kuwa na umoja katika wakati wa Gideon (Taluti) miaka mia mbili kabla ya Nabii Daudi, na umoja huo ukakamilika katika wakati wa Nabii Daudi, hata nguvu ya maadui wa wana wa Israeli ikavunjika katika wakati wake.

Aya 249. *Taabuut.* Watu wengine wamefikiri kuwa neno hili *Taabuut* kusudi lake ni sanduku ambayo habari zake zimeelezwa katika kisa cha Saul katika Biblia. Lakini fikira hiyo si

تَحْمِلُهُ الْمَلٰٓئِكَةُ ؕ اِنَّ فِيْ ذٰلِكَ لَاٰيَةً لَّكُمْ اِنْ كُنْتُمْ مُّؤْمِنِيْنَ ﴿۲۴۸﴾ ع ۳۲ ۱۲

ya yale waliyoyaacha watu wa Musa na watu wa Harun, wakiuchukua Malaika. Bila shaka katika hayo imo Ishara kwenu ikiwa ninyi ni waaminio.

FUNGU 33

فَلَمَّا فَصَلَ طَالُوْتُ بِالْجُنُوْدِ ۙ قَالَ اِنَّ اللّٰهَ مُبْتَلِيْكُمْ بِنَهَرٍ ۚ فَمَنْ شَرِبَ مِنْهُ فَلَيْسَ مِنِّيْ ۚ وَمَنْ لَّمْ يَطْعَمْهُ فَاِنَّهٗ مِنِّيْٓ اِلَّا مَنِ اغْتَرَفَ غُرْفَةً بِيَدِهٖ ۚ فَشَرِبُوْا مِنْهُ اِلَّا قَلِيْلًا مِّنْهُمْ ؕ فَلَمَّا جَاوَزَهٗ هُوَ وَالَّذِيْنَ اٰمَنُوْا مَعَهٗ ۙ قَالُوْا لَا طَاقَةَ لَنَا الْيَوْمَ بِجَالُوْتَ وَجُنُوْدِهٖ ؕ قَالَ الَّذِيْنَ يَظُنُّوْنَ اَنَّهُمْ مُّلٰقُوا اللّٰهِ ۙ كَمْ مِّنْ فِئَةٍ قَلِيْلَةٍ غَلَبَتْ فِئَةً كَثِيْرَةًۢ بِاِذْنِ اللّٰهِ ؕ وَاللّٰهُ مَعَ الصّٰبِرِيْنَ ﴿۲۴۹﴾

250. Basi Taluti alipoondoka na majeshi, akasema: Hakika Allah Atawajaribuni kwa mto, basi atakayekunywa humo si pamoja nami, na asiyeyanywa bila shaka yu pamoja nami, ila atakayeteka kwa kiasi cha kujaza kitanga cha mkono wake. Lakini walikunywa humo isipokuwa wachache tu miongoni mwao. Basi alipovuka yeye na walioamini pamoja naye, wakasema: Leo hatumwezi Jaluti na majeshi yake. Wakasema wale wenye yakini ya kukutana na Mola wao: Makundi mangapi madogo yameyashinda makundi makubwa kwa idhini ya Allah! Na Allah Yu pamoja na wafanyao subira.

وَلَمَّا بَرَزُوْا لِجَالُوْتَ وَجُنُوْدِهٖ قَالُوْا رَبَّنَآ اَفْرِغْ عَلَيْنَا صَبْرًا وَّ ثَبِّتْ اَقْدَامَنَا وَانْصُرْنَا عَلَى الْقَوْمِ الْكٰفِرِيْنَ ﴿۲۵۰﴾

251. Na walipotoka kupambana na Jaluti na majeshi yake, wakasema: Mola wetu, tumiminie subira, na Uiimarishe miguu yetu, na Utusaidie juu ya watu makafiri.

---

sawa. Katika lugha ya Kiarabu neno *Taabuut* maana yake pia ni moyo (Mufradat na Lane). Basi hapa Allah Anaahidi kuwa watu wa Gideon watapewa mioyo mizuri yenye utawa na ujasiri. Kama si hivi, basi sanduku ya Saul haikumfaa hata kidogo; haikuweza kuwalinda wana wa Israeli wala hikuweza kujilinda nafsi yake. Hivyo *Taabuut* hiyo siyo sanduku la chuma au la miti bali mradi wake ni moyo wenye ujasiri na wema.

Aya 250. *Asiyeyanywa bila shaka yu pamoja nami.* Utii na kujizuia ni shina la ufaulu wa kila namna. Allah aliwajaribu watu wa Gideon kwa maji; waliojizuia na kutii wakashinda, na waasi wakashindwa.

Makundi mangapi madogo yameyashinda makundi makubwa. Maneno haya ya Allah ni somo lenye thamani kwa ajili ya waaminio; wasiogope wingi wa maadui. bali wamtegemee yeye Anayeweza kuwasaidia.

Aya 251. *Jaaluti na majeshi yake. Jaaluut* mradi wake si mtu mmoja, bali taifa la watu.

252. Basi wakawashinda kwa idhini ya Allah; na Daud akamwua Jaluti, na Allah Akampa ufalme na hekima na Akamfundisha Aliyopenda. Na kama Allah Asingaliwazuia watu, baadhi yao kwa wengine, kwa yakini ardhi ingaliharibika; lakini Allah ni Mwenye kuwafadhili walimwengu.

فَهَزَمُوْهُمْ بِاِذْنِ اللّٰهِ ۙ وَقَتَلَ دَاوٗدُ
جَالُوْتَ وَاٰتٰىهُ اللّٰهُ الْمُلْكَ وَالْحِكْمَةَ
وَعَلَّمَهٗ مِمَّا يَشَآءُ ؕ وَلَوْلَا دَفْعُ اللّٰهِ النَّاسَ
بَعْضَهُمْ بِبَعْضٍ ۙ لَّفَسَدَتِ الْاَرْضُ
وَلٰكِنَّ اللّٰهَ ذُوْ فَضْلٍ عَلَى الْعٰلَمِيْنَ ﴿۲۵۱﴾

253. Hizi ndizo Aya za Allah Tunazokusomea kwa haki; na bila shaka wewe u miongoni mwa waliotumwa.

تِلْكَ اٰيٰتُ اللّٰهِ نَتْلُوْهَا عَلَيْكَ بِالْحَقِّ ؕ
وَاِنَّكَ لَمِنَ الْمُرْسَلِيْنَ ﴿۲۵۲﴾

JUZU 3

254. Hao Mitume Tumewafadhili baadhi yao zaidi kuliko wengine; miongoni mwao wako ambao Allah Alisema nao sana, na wengine wao akawapandisha daraja. Na Isa mwana wa Mariamu Tukampa Ishara zilizo wazi, na Tukamsaidia kwa roho takatifu. Na kama Allah Angalipenda wasingalipigana wao kwa wao baada ya kuwafikia Ishara zilizo wazi, lakini walihitilafiana. Kwa hiyo wako miongoni mwao walioamini, na

تِلْكَ الرُّسُلُ فَضَّلْنَا بَعْضَهُمْ عَلٰى
بَعْضٍ ۘ مِنْهُمْ مَّنْ كَلَّمَ اللّٰهُ وَرَفَعَ
بَعْضَهُمْ دَرَجٰتٍ ؕ وَاٰتَيْنَا عِيْسَى ابْنَ
مَرْيَمَ الْبَيِّنٰتِ وَاَيَّدْنٰهُ بِرُوْحِ الْقُدُسِ ؕ
وَلَوْ شَآءَ اللّٰهُ مَا اقْتَتَلَ الَّذِيْنَ مِنْۢ
بَعْدِهِمْ مِّنْۢ بَعْدِ مَا جَآءَتْهُمُ الْبَيِّنٰتُ
وَلٰكِنِ اخْتَلَفُوْا فَمِنْهُمْ مَّنْ اٰمَنَ

Na 'majeshi yake' mradi ni wasaidizi wa watu hao. Biblia inaeleza habari za Jaaluut kwa jina la Wamidiani ambao waliwasumbua sana Waisraeli na kuwateka nyara na kuiharibu nchi yao kwa miaka kadha wa kadha (waamuzi 6:1-6). Waamaleki pamoja na makabila yote ya upande wa mashariki waliwasaidia Wamidiani katika mashambulio haya (Waamuzi 6:3), nao ndio majeshi ambayo yametajwa katika Aya hii.

Aya 252. *Mungu Asingaliwazuia watu, baadhi yao kwa wengine.* Hapa Allah Anaeleza kuwa kusudi la vita liwe kusimamisha raha na amani katika dunia, si kwa ajili ya kuchafua amani ya dunia.

Aya 254. *Tumewafadhili baadhi yao zaidi kuliko wengine.* (1) Baadhi ya Manabii walipewa Sheria mpya na wengine walipewa sahifa ndogo ndogo na wengine waliteremshiwa ufunuo tu

وَ مِنۡهُمۡ مَّنۡ كَفَرَ ؕ وَلَوۡ شَآءَ اللّٰهُ مَا
اقۡتَتَلُوۡا ۫ وَلٰكِنَّ اللّٰهَ يَفۡعَلُ مَا يُرِيۡدُ ﴿۲۵۳﴾ ع ۳۳

wengine miongoni mwao waliokufuru. Na kama Allah Angalipenda, wasingalipigana; lakini Allah Hufanya Anavyotaka.

FUNGU 34

يٰۤاَيُّهَا الَّذِيۡنَ اٰمَنُوۡۤا اَنۡفِقُوۡا مِمَّا رَزَقۡنٰكُمۡ
مِّنۡ قَبۡلِ اَنۡ يَّاۡتِىَ يَوۡمٌ لَّا بَيۡعٌ فِيۡهِ وَلَا خُلَّةٌ
وَّ لَا شَفَاعَةٌ ؕ وَالۡكٰفِرُوۡنَ هُمُ
الظّٰلِمُوۡنَ ﴿۲۵۴﴾

255. Enyi mlioamini, toeni katika vile Tulivyowapeni kabla haijafika Siku ambayo haitakuwa na biashara, wala urafiki, wala uombezi; na waliokufuru ndio wadhalimu.

---

bila kupewa Kitabu cho chote. (2) Baadhi yao walipelekwa kwa watu wa mji mmoja tu, wengine kwa taifa moja na wengine kwa mataifa mengi. (3) Baadhi ya Mitume walipata wafuasi wengi katika maisha yao na wengine hawakufanikiwa sana. (4) Baadhi ya Manabii walipata ufalme wa dunia pamoja na Unabii na wengine hawakupata ufalme. (5) Tena katika kumkurubia Allah vilevile Mitume wana vyeo mbalimbali. Mathalan, katika usiku wa Miiraji Mtume s.a.w. aliwaona Manabii katika mbingu mbalimbali na yeye mwenyewe alipandishwa hata mbingu ya saba (Bukhari), pia tazama sura 53:5-19. Na kadhalika katika *Israa* Mtume Muhammad *s.a.w.* aliwasalisha Manabii wote katika *Bait-ul-Mukaddas.* Na hii yote inaonyesha kuwa yeye aliwapita Manabii wote katika cheo, na kwa vile ni yeye peke yake aliyetumwa kwa dunia nzima (sura 25:2 ; 7:159 ; Bukhari).

Aya hii pia yaweza kutafsiriwa kwa kuweka alama ya kupumzika baada ya neno *min hum* na siyo kabla yake. Kwa njia hii tafsiri itasomeka na kueleweka kwa urahisi zaidi na itatiririka kama ifuatavyo: Hao Mitume ambao miongoni mwao wako Tuliowainua daraja juu ya wengine, Allah Alisema nao na Akawapandisha baadhi yao madaraja ya vyeo.

Padre Dale anaona Aya hii haipatani na Aya 286 inayosema "Hatufanyi tofauti baina ya mmoja wa Mitume wake." Hebu tufikirie Aya ile tuone kama padre huyo anasema kweli. Aya inasema hivi: "Wote wamemwamini Allah, na Malaika Wake na Vitabu Vyake na Mitume Wake; (nao husema), Sisi hatufanyi tofauti baina ya mmoja wa Mitume Wake." Kila mtu mwenye maoni safi atafahamu ya kwamba Aya hii inatoa kanuni ya kuwaamini Mitume wote bila kumkataa hata mmoja; haisemi ya kuwa Manabii wote wako sawa katika vyeo. Padre ameshindwa kufahamu jambo hilo lililo dogo sana. Qur'an inafundisha kuwatukuza sana Manabii, wala sivyo kama alivyosema Yesu, "Wote walionitangulia ni wezi na wanyang'anyi" (Yohana 10:8). Mtu mwenye itikadi ya namna hii akishindwa kufahamu uzuri wa kanuni ya kuamini Manabii wote wa Allah, si kosa lake. Zaidi ya hayo kusema, hatutofautishi kati ya Mitume Wake ni usemi unaotakiwa waaminio waseme, na kuwafadhili Mitume baadhi yao kuliko wengine ni tendo la Allah.

Miongoni mwao wako ambao Allah Alisema nao. Sio mradi wake ya kuwa Mitume wengine Allah hakusema nao, au kwamba kuna Mitume asiowainua cheo. Maneno haya yametumiwa kuonyesha ya kuwa kuna namna mbili za Mitume. (1) Mitume wanaoleta Sheria; (2) Mitume wale ambao Utume wao umo katika kunyanyuliwa daraja zao. Neno "kusema" limetumiwa kuonyesha namna maalumu ya kusema, yaani wahyi unaoleta Sheria mpya.

Tukamsaidia kwa roho takatifu. Tazama sura 2:88.

256. Allah hakuna aabudiwaye ila Yeye Mwenye uzima, Mhifadhi wa milele; kusinzia hakumshiki wala kulala. Ni Vyake vilivyomo mbinguni na vilivyomo ardhini. Ni nani awezaye kuombea mbele Yake bila ya idhini Yake? Anayajua yaliyo mbele yao na yaliyo nyuma yao; wala hawawezi kujua cho chote katika elimu Yake ila yale Anayoyapenda. Enzi Yake imezienea mbingu na ardhi; na kuvilinda hivyo hakumchoshi, na Yeye ndiye Aliye juu, Mkuu.

اَللّٰهُ لَآ اِلٰهَ اِلَّا هُوَ ۚ اَلْحَیُّ الْقَیُّوْمُ ۚ لَا
تَاْخُذُهٗ سِنَةٌ وَّلَا نَوْمٌ ؕ لَهٗ مَا فِی السَّمٰوٰتِ
وَمَا فِی الْاَرْضِ ؕ مَنْ ذَا الَّذِیْ یَشْفَعُ عِنْدَهٗۤ
اِلَّا بِاِذْنِهٖ ؕ یَعْلَمُ مَا بَیْنَ اَیْدِیْهِمْ وَمَا
خَلْفَهُمْ ۚ وَلَا یُحِیْطُوْنَ بِشَیْءٍ مِّنْ عِلْمِهٖۤ
اِلَّا بِمَا شَآءَ ۚ وَسِعَ كُرْسِیُّهُ السَّمٰوٰتِ
وَالْاَرْضَ ۚ وَلَا یَـُٔوْدُهٗ حِفْظُهُمَا ۚ وَهُوَ
الْعَلِیُّ الْعَظِیْمُ ﴿۲۵۶﴾

Aya 256. Aya hii inaitwa, *Aayat-ul-Kursii,* na ni moja katika aya tukufu sana, na inaeleza vizuri umoja wa Allah na sifa Zake kubwa kubwa. Mtume *s.a.w.* alisema, *Aayat-ul-Kursii* ndiyo iliyoinuka kabisa katika Qur'an (Muslim). Neno *Kursiyu* kimsingi lina maana ya kiti cha mamlaka au enzi. Maana hii ya neno hili ina matumizi mapana na inagubika siyo tu kielimu bali pia mahitaji mengine ya kiserikali.

Ni nani awezaye kuombea. Sababu ambayo hakuna mtu ye yote pasipo ruhusa ya Allah anayeweza kumwombea mtu mwingine ni kwamba hakuna ye yote ajuaye yaliyomo katika mioyo ya watu; ndipo ikawa hakuna mwenye makamo ya kumwombea mwingine. Allah tu ndiye Ajuaye siri za mioyo ya watu, hivyo hakutakuwa na kuombeana ila kwa ruhusa Yake, maana Yeye peke yake ndiye Ajuaye ni nani anayestahili uombezi.

Padre Dale aliposoma Aya hii uzuri wake ulimvuta moyo. Lakini kwa kuwa anaichukia Islam alitaka Aya kama hii ingelipatikana katika Vitabu vya Kikristo. Anaandika. "Yafaa kuwasomea Waislamu Zaburi cxxi na Isaya xl:27, etc, wajue ya kuwa maneno mazuri kama haya, au mazuri zaidi yaliandikwa miaka elfu kabla hajazaliwa Muhammad" (Tafsiri yake ya Qur'an uk. 558).

Tulistaajabu sana kwa sababu gani Bwana Dale hakupata Aya kama ile katika Injili ambamo yamo maneno mazuri. Kama Yesu Kristo angemsifu Mungu kwa sifa zilizo kubwa mno, Bwana Dale hangesumbuka kutafuta mfano wa Aya hii katika vyuo vya Manabii wa zamani, hasa katika Zaburi ya Daudi ambaye haaminiwi kama Nabii na Wakristo wengine.

Padre Dale alidhani labda Waislamu watatishwa na majina ya Vitabu vya Biblia na watatosheka na aliyoyaandika. Kwa hiyo twataka kueleza kidogo aya zile za Biblia na kuzilinganisha na *Aayat-ul-Kursii* kwa kifupi:-

1. Daudi na Isaya wanasema, Mungu aliumba nchi na mbingu. Lakini *Aayat-ul-Kursii* inafundisha, "Ni vyake vilivyomo mbinguni na vilivyomo ardhini," yaani mamlaka ya Allah yameenea juu ya kila kilichomo mbinguni na ardhini.

2. Zaburi inasema, Mungu "Hataacha mguu wako uondolewe." Lakini Qur'an inabainisha sifa ya Mhifadhi wa milele. Inaonekana waziwazi ya kwamba 'Mhifadhi wa milele' inachukua vitu vyote vilivyokuwa zamani, vilivyoko sasa, na vitakavyokuwa baadaye. Si mguu mmoja tu. Aya ya nne ya Zaburi hiyo inampa Allah sifa ya "Mlinzi wa Israeli." Je Mungu ni Mlinzi wa Israeli tu au ni Mhifadhi wa vitu vyote na watu wote?

3. Isaya inasema, "Mungu hadhoofiki wala hachoki" (40:28). Ni kweli na Qur'an pia inasema

257. Hakuna karaha katika dini; hakika uongofu umekwisha pambanuka katika upotevu; basi anayemkataa Shetani na kumwamini Allah, bila shaka yeye ameshika kishikio kigumu kisichovunjika; na Allah ni Asikiaye, Ajuaye.

لَآ اِكۡرَاهَ فِى الدِّيۡنِ ۙ قَدۡ تَّبَيَّنَ الرُّشۡدُ مِنَ
الۡغَىِّ ۚ فَمَنۡ يَّكۡفُرۡ بِالطَّاغُوۡتِ وَيُؤۡمِنۡ
بِاللّٰهِ فَقَدِ اسۡتَمۡسَكَ بِالۡعُرۡوَةِ الۡوُثۡقٰى ۗ
لَا انۡفِصَامَ لَهَا ؕ وَاللّٰهُ سَمِيۡعٌ عَلِيۡمٌ ﴿۲۵۶﴾

258. Allah ni mlinzi wa wale walioamini: Huwatoa katika giza kuwapeleka kwenye mwangaza; lakini waliokufuru walinzi wao ni mashetani, huwatoa katika mwangaza na kuwaingiza kwenye giza. Hao ndio watu wa Motoni, humo watakaa.

اَللّٰهُ وَلِىُّ الَّذِيۡنَ اٰمَنُوۡا ۙ يُخۡرِجُهُمۡ مِّنَ
الظُّلُمٰتِ اِلَى النُّوۡرِ ؕ وَالَّذِيۡنَ كَفَرُوۡۤا
اَوۡلِيٰٓـئُهُمُ الطَّاغُوۡتُ ۙ يُخۡرِجُوۡنَهُمۡ مِّنَ
النُّوۡرِ اِلَى الظُّلُمٰتِ ؕ اُولٰٓـئِكَ اَصۡحٰبُ
النَّارِ ۚ هُمۡ فِيۡهَا خٰلِدُوۡنَ ﴿۲۵۷﴾ ع ۳۴/۲

---

hivyo. Lakini mbona chuo cha Mwanzo 2:2 kinasema ya kwamba siku ya saba Mungu alipumzika? Je, maneno ya Mungu yanapinzana? Qur'an haisemi Allah alichoka au alipumzika.

Kadhalika, ingawa Zaburi 121:4 inasema Mungu hasinzii wala halali, katika Zaburi 44:23 Daudi anamwambia Mungu "Amka! kwa nini umelala, ewe Bwana?" Lakini hutakuta mahali po pote katika Qur'an maneno yanayopinzana na *Aayat-ul-Kursii* au Aya nyinginezo.

4. Tena *Aayat-ul-Kursii* inatangaza, "Hakuna mwingine aabudiwaye ila yeye." Na Biblia imechanganya pamoja mafunzo ya Umoja wa Mungu na ushirikina. Zaburi hiyo hiyo inayomsifu Mungu inasema. "Nami nimesema, Ndinyi miungu" (82:6). Na Wakristo wanaamini Yesu kuwa Mungu na baadhi yao wanawaomba mama yake, Mariamu na watakatifu wengine na wanaleta sehemu mbalimbali za Biblia kuhakikisha maneno yao. Kitabu kama hiki hakistahili kuletwa mbele ya Qur'an.

Kama Aya sawa na *Aayat-ul-Kursii* ingepatikana katika Biblia, Padre Dale angesema, Muhammad alichukua mafundisho hayo toka Biblia. Lakini kwa kuwa haimo hakuweza kusema hayo.

Aya 257. *Hakuna karaha katika dini.* Aya hii inawafunza Waislamu kwa maneno yaliyo wazi kabisa na yenye nguvu kwamba wasisilimishe watu kwa nguvu. Aya inawatia vumbi machoni watu wanaoisingizia dini ya Kiislamu kuwa inaruhusu kuwaingiza watu katika dini kwa nguvu. Imani ni kitu cha hiyari. Hakuna nguvu inayoweza kuingiza imani katika moyo wa mtu.

Allah amesema, "Na useme: Kweli hii imetoka kwa Mola wenu, basi anayependa aikubali, na anayependa basi aikatae" (sura 18:30). Na tena amesema. "Sema: Enyi watu ! hakika haki imekwisha wafikieni kutoka kwa Mola wenu, basi anayeongoka, anaongoka kwa faida ya nafsi yake, na anayepotea, basi anapotea kwa hasara ya nafsi yake, na mimi si mlinzi juu yenu" (sura 10:109). Aya kama hizi zinazoonyesha kuwa dini ya Kiislamu haikuenezwa ila kwa njia nzuri zisizo karaha ni nyingi katika Qur'an. Ni kweli Waislamu walipigana vita. Lakini si kwa sababu ya kutaka kueneza dini. Vita walizopigana Waislamu zilikuwa kwa kujikinga na kusimamisha uhuru duniani, kwa kuwazuia watu wabaya waliokuwa hawataki watu wafuate dini kwa hiyari zao. Habari za vita za Waislamu zitaelezwa chini ya Aya zinazohusu. Pia tazama sura 22:40.

FUNGU 35

اَلَمْ تَرَ اِلَى الَّذِیْ حَآجَّ اِبْرٰهٖمَ فِیْ رَبِّهٖۤ
اَنْ اٰتٰىهُ اللّٰهُ الْمُلْكَ ۘ اِذْ قَالَ اِبْرٰهٖمُ رَبِّیَ
الَّذِیْ یُحْیٖ وَ یُمِیْتُ ۙ قَالَ اَنَا اُحْیٖ
وَ اُمِیْتُ ؕ قَالَ اِبْرٰهٖمُ فَاِنَّ اللّٰهَ یَاْتِیْ
بِالشَّمْسِ مِنَ الْمَشْرِقِ فَاْتِ بِهَا مِنَ
الْمَغْرِبِ فَبُهِتَ الَّذِیْ كَفَرَ ؕ وَ اللّٰهُ
لَا یَهْدِی الْقَوْمَ الظّٰلِمِیْنَ ۝۲۵۸

259. Je, hukumwona yule aliyehojiana na Ibrahimu juu ya Mola wake kwa sababu Allah Alimpa ufalme? Ibrahimu aliposema: Mola wangu ni Yule Ambaye Huhuisha na Hufisha, yeye akasema: Mimi pia nahuisha na kufisha. Ibrahimu akasema: Hakika Allah Hulileta jua toka mashariki, basi wewe ulilete toka magharibi, ndipo akapigwa butwaa yule aliyekufuru; na Allah Hawaongozi watu wadhalimu.

اَوْ كَالَّذِیْ مَرَّ عَلٰی قَرْیَةٍ وَّ هِیَ خَاوِیَةٌ
عَلٰی عُرُوْشِهَا ۚ قَالَ اَنّٰی یُحْیٖ هٰذِهِ اللّٰهُ بَعْدَ
مَوْتِهَا ۚ فَاَمَاتَهُ اللّٰهُ مِائَةَ عَامٍ ثُمَّ
بَعَثَهٗ ؕ قَالَ كَمْ لَبِثْتَ ؕ قَالَ لَبِثْتُ یَوْمًا

260. Au kama yule aliyepita katika mji uliokuwa umeangamia; akasema: Allah Atauhuisha vipi (mji) huu baada ya kufa kwake? Basi Allah Akamweka katika hali kama ya mauti kwa miaka

---

Aya 259. Aliyehojiana na Nabii Ibrahimu ni mfalme Namrud (Nimrod). Nabii Ibrahimu alikuwa adui wa ibada ya masanamu, na alihubiri kwa kasi kuyalaumu. Siku moja aliitia moto nyumba iliyokuwa na masanamu ya miti. Siku nyingine aliyavunjavunja masanamu na akayatia moto. Hapo alishtakiwa akaletwa mbele ya mfalme Namrud (Mwanzo 10:8, 9 na Jewish Encyclopaedia). Huyu Namrud pia alikuwa anaabudiwa na watu kama naibu wa miungu wao. Inaonekana mfalme alimkaripia Ibrahimu kwa kitisho cha kumwua. Nabii Ibrahimu kwa uhodari sana akamjibu ya kuwa hawezi kumdhuru, kwani ni Allah anayetoa uhai na kifo. Kwa kuwa mfalme alijidai yu mungu, alijibu kwa hamaki kuwa ni yeye anayehuisha na kufisha. Ibrahimu alijibu ya kwamba Namrudi na watu wake walikuwa wakisadiki ya kwamba uhai wote ulitegemea juu ya jua (ambalo lilikuwa ndilo mungu wao mkubwa). Hivyo kama ni kweli mfalme ndiye aliyeshika uhai na mauti itakuwa na maana ya kuwa hata jua lilikuwa chini ya nguvu ya mfalme, na ya kuwa uwezo kamili ambao Namrud na watu wake walilisifia jua ilikuwa upuuzi mtupu. Hapo Ibrahimu akamwambia mfalme alirudishe jua toka mashariki mpaka magharibi (yaani aliondoe), maana katika hali hiyo jua lisingekubaliwa kuwa ndilo lenye mamlaka. Mfalme akakwama. Hakuweza kusema kwamba hana uwezo wa kulirudisha jua maana angejiumbua. Kadhalika hakuweza kusema kuwa ni yeye anayelifanya jua kuchomoza mashariki na kutua magharibi, maana watu waliliona jua kuwa mungu mkubwa, hata zaidi kuliko mfalme. Na kama angedai kuwa na uwezo kuliko jua, watu wake lazima wangeumuka kumkasirikia. Hapo akafumbwa mdomo asijue la kujibu.

Aya 260. *Aliyepita katika mji,* ni Nabii Ezekiel, na mji uliokuwa umeharibiwa ni Jerusalem uliposhambuliwa na mfalme Bukhtanassar (Nebuchadnezzar) kwanza katika mwaka

اَوْ بَعْضَ يَوْمٍ ؕ قَالَ بَلْ لَّبِثْتَ مِائَةَ
عَامٍ فَانْظُرْ اِلٰى طَعَامِكَ وَشَرَابِكَ لَمْ
يَتَسَنَّهْ ۚ وَانْظُرْ اِلٰى حِمَارِكَ وَلِنَجْعَلَكَ
اٰيَةً لِّلنَّاسِ وَانْظُرْ اِلَى الْعِظَامِ كَيْفَ
نُنْشِزُهَا ثُمَّ نَكْسُوْهَا لَحْمًا ؕ فَلَمَّا تَبَيَّنَ
لَهٗ ۙ قَالَ اَعْلَمُ اَنَّ اللّٰهَ عَلٰى كُلِّ شَىْءٍ
قَدِيْرٌ ﴿٢٦٠﴾

mia, kisha Akamfufua.Akasema: Umekaa muda gani (katika hali hii)? Akasema: Nimekaa siku moja au sehemu ya siku. (Allah) Akasema: Bali umekaa miaka mia, nawe tazama chakula chako na kinywaji chako, havijaharibika. Na mtazame punda wako. Na ili tukufanye uwe Ishara kwa watu, na uitazame mifupa jinsi Tunavyoikuza, kisha Tunaivisha nyama. Basi yalipombainikia, akanena: Najua kwamba Allah ni Mwenye uwezo juu ya kila kitu.

وَاِذْ قَالَ اِبْرٰهٖمُ رَبِّ اَرِنِىْ كَيْفَ تُحْىِ
الْمَوْتٰى ؕ قَالَ اَوَلَمْ تُؤْمِنْ ؕ قَالَ بَلٰى
وَلٰكِنْ لِّيَطْمَئِنَّ قَلْبِىْ ؕ قَالَ فَخُذْ اَرْبَعَةً
مِّنَ الطَّيْرِ فَصُرْهُنَّ اِلَيْكَ ثُمَّ اجْعَلْ عَلٰى
كُلِّ جَبَلٍ مِّنْهُنَّ جُزْءًا ثُمَّ ادْعُهُنَّ يَاْتِيْنَكَ
سَعْيًا ؕ وَاعْلَمْ اَنَّ اللّٰهَ عَزِيْزٌ حَكِيْمٌ ﴿٢٦١﴾ ع ٣٤

261. Na (kumbuka) Ibrahimu aliposema: Mola wangu, nionyeshe jinsi Unavyowafufua wafu. (Allah) Akasema: Je, hujaamini? Akasema: Naam (nimeamini), lakini ili moyo wangu utulie. Akasema: Basi chukua ndege wanne na uwazoeshe kwako, kisha uwaweke juu ya kila jabali mmoja wao, kisha uwaite, watakujia mbio. Na jua ya kwamba Allah ni Mwenye ushindi kamili, Mwenye hekima.

---

597 B.C. na tena katika 587 B.C. na mwishoni mji uliangamizwa kabisa na jemadari wake katika mwaka 586 B.C. mwaka ambao Nabii Ezekiel alipoona njozi hiyo ya kufa miaka 100.

Allah Akamfisha kwa miaka mia. Siyo maana yake Nabii Ezekiel alikufa hasa akafufuliwa, ila ni desturi ya Qur'an kueleza habari za ndoto kana kwamba ni mambo yaliyotokea vivi hivi, kama ilivyoelezwa ndoto ya Nabii Yusuf. Njozi hiyo mradi wake ulikuwa kumjulisha Nabii Ezekiel ya kuwa maanguko ya mji wa Yerusalem yatadumu kwa miaka 100 kisha mji utajengwa tena; na ndivyo ilivyotokea.

Aya 261. *Fasurhunna ilaika.* Maneno haya yametafsiriwa "Uwazoeshe kwako," siyo "uwakatekate na uwakoroge", kama walivyotafsiri baadhi ya watu.

FUNGU 36

مَثَلُ الَّذِيْنَ يُنْفِقُوْنَ اَمْوَالَهُمْ فِيْ سَبِيْلِ
اللّٰهِ كَمَثَلِ حَبَّةٍ اَنْۢبَتَتْ سَبْعَ سَنَابِلَ فِيْ كُلِّ
سُنْۢبُلَةٍ مِّائَةُ حَبَّةٍ ؕ وَاللّٰهُ يُضٰعِفُ لِمَنْ
يَّشَآءُ ؕ وَاللّٰهُ وَاسِعٌ عَلِيْمٌ ﴿٢٦١﴾

262. Mfano wa wale wanaotoa mali zao katika njia ya Allah, ni kama mfano wa punje moja itoayo masuke saba, katika kila suke mna punje mia. Na Allah Humzidishia Amtakaye; na Allah ni Mwenye wasaa, Mwenye kujua.

اَلَّذِيْنَ يُنْفِقُوْنَ اَمْوَالَهُمْ فِيْ سَبِيْلِ اللّٰهِ
ثُمَّ لَا يُتْبِعُوْنَ مَآ اَنْفَقُوْا مَنًّا وَّلَآ اَذًى ۙ
لَّهُمْ اَجْرُهُمْ عِنْدَ رَبِّهِمْ ۚ وَلَا خَوْفٌ
عَلَيْهِمْ وَلَا هُمْ يَحْزَنُوْنَ ﴿٢٦٢﴾

263. Wale wanaotoa mali zao katika njia ya Allah kisha hawafuatishii waliyoyatoa kwa masimbulizi wala udhia, wao wana ujira wao kwa Mola wao, wala haitakuwa hofu juu yao wala hawatahuzunika.

قَوْلٌ مَّعْرُوْفٌ وَّمَغْفِرَةٌ خَيْرٌ مِّنْ صَدَقَةٍ
يَّتْبَعُهَآ اَذًى ؕ وَاللّٰهُ غَنِيٌّ حَلِيْمٌ ﴿٢٦٣﴾

264. Kauli njema na msamaha ni bora kuliko sadaka inayofuatishwa na udhia; na Allah ndiye Mkwasi, Avumiliaye.

يٰٓاَيُّهَا الَّذِيْنَ اٰمَنُوْا لَا تُبْطِلُوْا صَدَقٰتِكُمْ
بِالْمَنِّ وَالْاَذٰى ۙ كَالَّذِيْ يُنْفِقُ مَالَهٗ رِئَآءَ
النَّاسِ وَلَا يُؤْمِنُ بِاللّٰهِ وَالْيَوْمِ الْاٰخِرِ ؕ
فَمَثَلُهٗ كَمَثَلِ صَفْوَانٍ عَلَيْهِ تُرَابٌ

265. Enyi mlioamini, msiharibu sadaka zenu kwa masimbulizi na udhia, kama yule anayetoa mali yake kwa kuwaonyesha watu, wala hamwamini Allah na siku ya Mwisho. Basi hali yake ni kama hali ya mwamba

---

Aya 262. *Mfano wa wale wanaotoa mali zao.* Padre Dale amemsingizia Mtume *s.a.w.* kuwa alisikia mfano huo wa mpanzi kwa Wakristo, akaupenyeza katika Qur'an. Kusudi lake ni kutaka kutia wasiwasi moyoni mwa msomaji wake kwamba Mtume *s.a.w.* hakuteremshiwa cho chote na Allah na maneno ya Qur'an ni hadithi tu alizozisikia kwa watu.

1. Twataka kujua kwanza, je, methali hiyo Yesu alifundishwa na nani? Kama alifundishwa na Mungu, basi je, Mungu hawezi kumfunzayo mwingine?

2. Watu wo wote wanaojua habari za kilimo hueleza watakapo mfano wa mpanzi, si Yesu peke yake.

3. Mfano uliotolewa na Qur'an haufanani na mfano uliotolewa na Injili. Qur'an imeleta mfano huo kwa kubainisha matokeo ya vitendo vya wale wanaotoa mali katika njia ya Allah; lakini Injili inaeleza jinsi neno la Mungu liingiavyo mioyoni mwa watu. Injili ya Marko inasema, "Mpanzi yule hulipanda neno" (4:14); na Luka anaandika, "Mbegu ni neno la Mungu" (8:11). Hivyo kutoa sadaka kunakosemwa na Qur'an, na kushika neno la Mungu kunakosemwa na Injili, ni habari mbili zilizo mbalimbali

4. Ujira ulioahidiwa katika mifano hiyo pia ni mbalimbali. Qur'an inaahidi kuotesha punje mia saba au zaidi katika mbegu moja. Lakini Injili inatoa punje mia moja tu toka mbegu moja..

فَاَصَابَهٗ وَابِلٌ فَتَرَكَهٗ صَلْدًا ؕ
لَا يَقْدِرُوْنَ عَلٰى شَیْءٍ مِّمَّا كَسَبُوْا ؕ
وَاللّٰهُ لَا يَهْدِی الْقَوْمَ الْكٰفِرِيْنَ ﴿۲۶۴﴾
وَمَثَلُ الَّذِيْنَ يُنْفِقُوْنَ اَمْوَالَهُمُ ابْتِغَآءَ
مَرْضَاتِ اللّٰهِ وَتَثْبِيْتًا مِّنْ اَنْفُسِهِمْ
كَمَثَلِ جَنَّةٍۭ بِرَبْوَةٍ اَصَابَهَا وَابِلٌ فَاٰتَتْ
اُكُلَهَا ضِعْفَيْنِ ۚ فَاِنْ لَّمْ يُصِبْهَا وَابِلٌ
فَطَلٌّ ؕ وَاللّٰهُ بِمَا تَعْمَلُوْنَ بَصِيْرٌ ﴿۲۶۵﴾
اَيَوَدُّ اَحَدُكُمْ اَنْ تَكُوْنَ لَهٗ جَنَّةٌ مِّنْ
نَّخِيْلٍ وَّاَعْنَابٍ تَجْرِیْ مِنْ تَحْتِهَا
الْاَنْهٰرُ ۙ لَهٗ فِيْهَا مِنْ كُلِّ الثَّمَرٰتِ ۙ
وَاَصَابَهُ الْكِبَرُ وَلَهٗ ذُرِّيَّةٌ ضُعَفَآءُ ۪
فَاَصَابَهَآ اِعْصَارٌ فِيْهِ نَارٌ فَاحْتَرَقَتْ ؕ
كَذٰلِكَ يُبَيِّنُ اللّٰهُ لَكُمُ الْاٰيٰتِ لَعَلَّكُمْ
تَتَفَكَّرُوْنَ ﴿۲۶۶﴾ ع

juu yake kuna udongo, kisha ikaufikia mvua kubwa na ikauacha mtupu; hawatakuwa na uwezo juu ya cho chote katika wanavyovichuma; na Allah hawaongozi watu makafiri.

266. Na mfano wa wale wanaotoa mali zao kwa kuitafuta radhi ya Allah na kujiimarisha wenyewe, ni kama mfano wa bustani iliyo mahali pa juu, ikaifikia mvua kubwa na ikaleta matunda yake mara dufu; na kama haifikiwi na mvua kubwa, basi hata umande (huitoshea); na Allah Anayaona mnayoyatenda.

267. Je, mmoja wenu anapenda kuwa na bustani ya mitende na mizabibu, ipitayo mito ndani yake, naye humo hupata matunda yake kila namna, na uzee ukamfikia, kisha ana watoto walio dhaifu, mara kimbunga chenye moto kiifikie, iungue? Hivi ndivyo Allah Anavyowabainishieni aya ili mpate kufikiri.

FUNGU 37

يٰۤاَيُّهَا الَّذِيْنَ اٰمَنُوْۤا اَنْفِقُوْا مِنْ طَيِّبٰتِ مَا
كَسَبْتُمْ وَمِمَّاۤ اَخْرَجْنَا لَكُمْ مِّنَ
الْاَرْضِ ۪ وَلَا تَيَمَّمُوا الْخَبِيْثَ مِنْهُ
تُنْفِقُوْنَ وَلَسْتُمْ بِاٰخِذِيْهِ اِلَّاۤ اَنْ تُغْمِضُوْا
فِيْهِ ؕ وَاعْلَمُوْۤا اَنَّ اللّٰهَ غَنِیٌّ حَمِيْدٌ ﴿۲۶۷﴾

268. Enyi mlioamini, toeni katika vitu vizuri mlivyovichuma, na katika vile tulivyowatoleeni katika ardhi, wala msikusudie (kutoa) vilivyo vibaya, ambavyo ninyi wenyewe msingevipokea isipokuwa kwa kutoviangalia, na jueni kwamba Allah ni Mkwasi, Asifiwaye.

Aya 268. Waaminio wanaambiwa ya kwamba watoe katika njia ya Allah, lakini watoe vitu vizuri na vilivyo safi. Wasifanye makusudi kuchagua vitu vyao vibaya-vibaya na vilivyochoka na kuvitoa sadaka.

اَلشَّيْطٰنُ يَعِدُكُمُ الْفَقْرَ وَيَاْمُرُكُمْ
بِالْفَحْشَآءِ ۚ وَاللّٰهُ يَعِدُكُمْ مَّغْفِرَةً مِّنْهُ
وَفَضْلًا ؕ وَاللّٰهُ وَاسِعٌ عَلِيْمٌ ﴿٢٦٨﴾

269. Shetani anawaogofisheni ufukara na anawaamuruni(kutenda) maovu, na Allah Anawaahidini msamaha utokao Kwake na ukarimu; na Allah ni Mwenye wasaa, Mwenye kujua.

يُّؤْتِي الْحِكْمَةَ مَنْ يَّشَآءُ ۚ وَمَنْ يُّؤْتَ
الْحِكْمَةَ فَقَدْ اُوْتِيَ خَيْرًا كَثِيْرًا ؕ وَمَا
يَذَّكَّرُ اِلَّآ اُولُوا الْاَلْبَابِ ﴿٢٦٩﴾

270. Humpa hekima Amtakaye, na aliyepewa hekima bila shaka amepewa heri nyingi; na hawazingatii nasaha ila wenye akili.

وَمَآ اَنْفَقْتُمْ مِّنْ نَّفَقَةٍ اَوْ نَذَرْتُمْ مِّنْ
نَّذْرٍ فَاِنَّ اللّٰهَ يَعْلَمُهٗ ؕ وَمَا لِلظّٰلِمِيْنَ
مِنْ اَنْصَارٍ ﴿٢٧٠﴾

271. Na cho chote mtoacho au nadhiri mnazoweka basi hakika Allah Anazijua; na kwa wadhalimu hawatakuwako wasaidizi.

اِنْ تُبْدُوا الصَّدَقٰتِ فَنِعِمَّا هِيَ ۚ وَاِنْ
تُخْفُوْهَا وَتُؤْتُوْهَا الْفُقَرَآءَ فَهُوَ خَيْرٌ
لَّكُمْ ؕ وَيُكَفِّرُ عَنْكُمْ مِّنْ سَيِّاٰتِكُمْ ؕ
وَاللّٰهُ بِمَا تَعْمَلُوْنَ خَبِيْرٌ ﴿٢٧١﴾

272. Kama mkizidhihirisha sadaka ni vizuri; na kama mkitoa kwa siri na kuwapa mafakiri, basi hiyo ni bora kwenu; na Atawaondoleeni mengi ya maovu yenu; na Allah daima Anazo habari za yale mnayoyatenda.

Aya 270. Fundisho hili la kutoa mchango na sadaka katika njia njema ni jambo la busara sana na ndiyo siri ya mainuko na kukua taifa la watu.

Aya 272. Islam imetumia busara sana kuruhusu namna zote mbili za kutoa sadaka, yaani, kutoa kwa dhahiri na kutoa kwa siri. Mtu akitoa sadaka waziwazi itakuwa anawafunza wengine kwa mfano wake ili nao wapate kumwiga. Kutoa kwa siri mara nyingi huwa ni bora, maana mtoaji hadhihirishi umaskini wa nduguze anaowapa sadaka na pia haitokei sana kuwa mtoaji ajivune.

Mapadre hujivunia sana mafundisho ya "Mwokozi" wao. Itafaa kulinganisha fundisho la Qur'an na fundisho la Injili juu ya jambo la sadaka. Katika Mattayo 6:1-4 mmeandikwa hivi, "Angalieni msitoe sadaka zenu mbele ya watu, kusudi mtazamwe nao . . . " Kutoa sadaka mbele ya watu ili kutazamwa nao si jambo jema, lakini je, mtu anapotoa sadaka mbele ya watu huwa na nia hiyo hiyo? Kwa kusema hivyo Injili imefunga mlango mmoja wa wema. Na Wakristo hasa ndio wako mbele sana katika kuonyesha na kuzitangaza sadaka zao. Katika makanisa na ndani ya mikutano, waalimu na watu wa makanisa wanatembeza makofia na mifuko kwa kuombaomba sadaka. Tamaa ya mali inawasahaulisha fundisho la Yesu Kristo. Ni wazi ya kwamba Qur'an imetoa mafundisho yaliyo bora kuliko mafundisho ya Injili, tena kamili kabisa. Katika vitendo vingi Wakristo wanafuata maagizo ya Qur'an, lakini jambo la ajabu ni hili ya kwamba wanamchukia Mtume Mtukufu aliyeleta mafundisho hayo.

لَيْسَ عَلَيْكَ هُدٰىهُمْ وَلٰكِنَّ اللّٰهَ يَهْدِيْ
مَنْ يَّشَآءُ ؕ وَمَا تُنْفِقُوْا مِنْ خَيْرٍ
فَلِاَنْفُسِكُمْ ؕ وَمَا تُنْفِقُوْنَ اِلَّا ابْتِغَآءَ
وَجْهِ اللّٰهِ ؕ وَمَا تُنْفِقُوْا مِنْ خَيْرٍ يُّوَفَّ
اِلَيْكُمْ وَاَنْتُمْ لَا تُظْلَمُوْنَ ﴿۲۷۲﴾

273. Si juu yako kuwaongoza; lakini Allah Humwongoza Amtakaye. Na mali yo yote muitoayo ni kwa (faida ya) nafsi zenu, wala hamtoi ila kwa kutafuta radhi ya Allah; na mali yo yote mtakayotoa mtarudishiwa sawasawa, wala hamtapunjwa,

لِلْفُقَرَآءِ الَّذِيْنَ اُحْصِرُوْا فِيْ سَبِيْلِ اللّٰهِ
لَا يَسْتَطِيْعُوْنَ ضَرْبًا فِي الْاَرْضِ ۫
يَحْسَبُهُمُ الْجَاهِلُ اَغْنِيَآءَ مِنَ التَّعَفُّفِ ۚ
تَعْرِفُهُمْ بِسِيْمٰهُمْ ۚ لَا يَسْـَٔلُوْنَ النَّاسَ
اِلْحَافًا ؕ وَمَا تُنْفِقُوْا مِنْ خَيْرٍ فَاِنَّ اللّٰهَ
بِهٖ عَلِيْمٌ ﴿۲۷۳﴾ ع ۳۷

274. Kwa (kuwapa) mafakiri waliozuiwa katika njia ya Allah, wasioweza kutembea huko na huko katika ardhi; mjinga anawadhania kuwa ni matajiri kwa sababu ya kujizuia (kuomba). Unawafahamu kwa alama zao; hawaombi watu kwa kung`ng`nia. Na mali yo yote mnayotoa, basi kwa yakini Allah Anaijua.

FUNGU 38

اَلَّذِيْنَ يُنْفِقُوْنَ اَمْوَالَهُمْ بِالَّيْلِ وَالنَّهَارِ
سِرًّا وَّ عَلَانِيَةً فَلَهُمْ اَجْرُهُمْ عِنْدَ
رَبِّهِمْ ۚ وَلَا خَوْفٌ عَلَيْهِمْ وَلَا هُمْ
يَحْزَنُوْنَ ﴿۲۷۴﴾

275. Wale watoao mali zao usiku na mchana, kwa siri na dhahiri, basi wana ujira wao kwa Mola wao; wala haitakuwa hofu juu yao wala hawatahuzunika.

اَلَّذِيْنَ يَاْكُلُوْنَ الرِّبٰوا لَا يَقُوْمُوْنَ اِلَّا
كَمَا يَقُوْمُ الَّذِيْ يَتَخَبَّطُهُ الشَّيْطٰنُ مِنَ
الْمَسِّ ؕ ذٰلِكَ بِاَنَّهُمْ قَالُوْٓا اِنَّمَا الْبَيْعُ مِثْلُ

276. Wale wanaokula riba, hawatasimama ila kama anavyosimama yule ambaye Shetani humpoozesha kwa kumshika. Hayo ni kwa sababu

Aya 273. *Mali yo yote mtakayotoa.* Neno la kiarabu lililotumika hapa kwa kutaja mali ni neno *khair* na maana yake ni "mali njema iliyochumwa kwa njia ya halali."

Aya 274. *Waliozuiwa katika njia ya Allah:* (1) Ni watu wanaojizuia mahali alipo mtu mtawa na hawaondoki alipo ili wasikie kila analolisema na waone kila analotenda na baadaye wawafikishie watu wengine elimu hiyo waliyochuma. Mfano ni wa Abu Huraira, aliyeingia dini ya Kiislamu miaka mitatu Mtume s.a.w. hajafariki, na toka hapo akakaa msikitini apate kuwa siku zote pamoja na Mtume *s.a.w.* (2) Ni Mwislamu ambaye Kwa sababu ya uadui wa makafiri amezuilika mahali na hana njia ya kupata matumizi.

Aya 276. *Riba* ni kila deni linalotanguliza kupata faida (Saghir), yaani kama mtu

الرِّبٰوا ۗ وَاَحَلَّ اللّٰهُ الْبَيْعَ وَحَرَّمَ الرِّبٰوا ؕ فَمَنْ جَآءَهٗ مَوْعِظَةٌ مِّنْ رَّبِّهٖ فَانْتَهٰى فَلَهٗ مَا سَلَفَ ؕ وَاَمْرُهٗۤ اِلَى اللّٰهِ ؕ وَمَنْ عَادَ فَاُولٰٓئِكَ اَصْحٰبُ النَّارِ ۚ هُمْ فِيْهَا خٰلِدُوْنَ ﴿۲۷۵﴾ يَمْحَقُ اللّٰهُ الرِّبٰوا وَيُرْبِى الصَّدَقٰتِ ؕ وَاللّٰهُ لَا يُحِبُّ كُلَّ كَفَّارٍ اَثِيْمٍ ﴿۲۷۶﴾

wamesema, Biashara ni kama riba tu; hali Allah Ameihalalisha biashara na kuiharamisha riba. Na aliyefikiwa na mawaidha kutoka kwa Mola wake, kisha akajizuia, basi yake ni yale yaliyokwisha pita, na shauri lake ni kwa Allah. Lakini anayerejea (kula riba), basi hao ndio watu wa Motoni, humo watakaa.

277. Allah Hufuta riba na Hukuza sadaka, na Allah Hampendi kila kafiri mkubwa na mtenda dhambi mkuu.

---

anamkopesha mwingine Shs. 500/= na anamwambia wakati wa kulipa atoe Shs. 5/= zaidi, au kabla ya kumaliza deni kila mwezi atoe Shs. 5/=, hii ndiyo riba. Na kama mtu anakwenda kukopa cho chote kwa mapatano ya namna hii pia ni riba. Ikumbukwe ya kuwa imekatazwa kutoa riba au kupokea riba.

Sababu kubwa ya kukataza riba ni kuwa si jambo lenye kupendeza kwamba mtu atake kujifaidisha katka taabu za nduguze. Wanaochukua riba wanakuwa na tamaa sana ya mali na wanakuwa na mioyo migumu isiyo huruma. Kadhalika kwa riba mali pole pole inaendelea kukusanyika katika mikono ya watu wachache, na kuzidi kuwaangusha chini maskini, na kwa njia hii maovu ya namna nyingi yanatokea duniani. Hivyo Allah hapendi jambo hili.

Qur'an ni Sheria ya kwanza iliyokataza kula riba. Biblia inakataza Mayahudi wasichukue riba kwa Mayahudi tu siyo kwa watu wengine (Kumbukumbu 23:19, 20). Hivyo inaonyesha ya kwamba, riba ni kitu kibaya waila isingeharimishwa kwa Mayahudi. Na pia inaonyesha kwamba Biblia ililetwa kwa kuwaongoza watu wa taifa maalumu tu, maana inatofautisha kati ya wana wa Israeli na watu wengine. Inaonekana kwamba Biblia si Sheria ya mwisho kwa wanadamu.

Injili iko kimya kabisa juu ya habari ya riba. Hivyo kwa kuwa Injili imekosa fundisho hilo lililo muhimu sana, Padre Dale amejaribu kuipinza Qur'an juu ya jambo la riba. Anasema, "na kadhalika fedha, nikikukopesha, siwezi kuitumia mwenyewe. Kwanini nisipewe faida kwa khasara yangu." (Tafsiri yake ya Qur'an uk. 559). Tazameni jinsi anavyopinga Biblia. Kama kuchukua riba ni jambo zuri, kwa sababu gani Myahudi alikatazwa kuchukua 'faida' hiyo kwa Myahudi mwenzake? Maadamu Wakristo wanafuata Biblia hawataweza kushambulia Qur'an. Padre Dale ingawa ni mtu wa dini ameshikwa sana na tamaa ya fedha. Kazi isiyomletea mali anaiona kama ni 'khasara'. Je, kumsaidia mwenzako na fedha au vyombo hata atimize haja yake si 'faida'? Kusaidiana na kupendana ndiyo faida kubwa na ndio Uislamu. Ukristo haumfikishi mtu katika daraja za juu za utu na ucha-Mungu ambako Uislamu unakusudia kumfikisha.

Ikumbukwe ya kwamba, kama mkopi wakati wa kulipa fedha aliyokopa amependa kumwongezea mfadhili wake cho chote, pasi na kuwa na mapatano yo yote kabla, basi kufanya hivyo si riba, na ndilo jambo lililopendelewa na Mtume *s.a.w.* Qur'an inasema, "Siyo malipo ya ihsani ila ihsani" (sura 55:61).

Aya 277. Aya hii inatoa maamuzi yaliyo wazi kabisa kwamba njia za uchumi ambazo misingi yake ni faida na riba ni lazima kabisa zitateketea ambapo zile chumi ambamo sadaka inatiliwa mkazo zitastawi.

278. Hakika wale walioamini na kufanya vitendo vizuri na kusimamisha Sala na kutoa Zaka, wao watapata ujira wao kwa Mola wao, wala haitakuwa hofu juu yao wala hawatahuzunika.

إِنَّ الَّذِينَ آمَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ
وَأَقَامُوا الصَّلَاةَ وَآتَوُا الزَّكَاةَ لَهُمْ
أَجْرُهُمْ عِندَ رَبِّهِمْ ۚ وَلَا خَوْفٌ عَلَيْهِمْ
وَلَا هُمْ يَحْزَنُونَ ﴿٢٧٧﴾

279. Enyi mlioamini! mcheni Allah, na acheni yaliyobakia katika riba, ikiwa mmeamini.

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا اتَّقُوا اللَّهَ وَذَرُوا مَا
بَقِيَ مِنَ الرِّبَا إِن كُنتُم مُّؤْمِنِينَ ﴿٢٧٨﴾

280. Na kama hamtafanya (hivyo), basi fahamuni mtakuwa na vita kutoka kwa Allah na Mtume Wake; na kama mkitubu, basi mtapata rasilimali zenu; hamtadhulumu wala hamtadhulumiwa.

فَإِن لَّمْ تَفْعَلُوا فَأْذَنُوا بِحَرْبٍ مِّنَ اللَّهِ
وَرَسُولِهِ ۖ وَإِن تُبْتُمْ فَلَكُمْ رُءُوسُ
أَمْوَالِكُمْ ۖ لَا تَظْلِمُونَ وَلَا تُظْلَمُونَ ﴿٢٧٩﴾

281. Na kama (mdaiwa) ana dhiki, basi (mdai) angoje mpaka amefarijika; na kama ninyi (mnaodai) mkiacha kama sadaka, ni bora kwenu, ikiwa mnajua.

وَإِن كَانَ ذُو عُسْرَةٍ فَنَظِرَةٌ إِلَىٰ مَيْسَرَةٍ ۚ
وَأَن تَصَدَّقُوا خَيْرٌ لَّكُمْ إِن كُنتُمْ
تَعْلَمُونَ ﴿٢٨٠﴾

282. Na ogopeni siku ambayo mtarudishwa kwa Allah, kisha kila mtu atapewa sawasawa aliyoyachuma, nao hawatadhulumiwa.

وَاتَّقُوا يَوْمًا تُرْجَعُونَ فِيهِ إِلَى اللَّهِ ثُمَّ
تُوَفَّىٰ كُلُّ نَفْسٍ مَّا كَسَبَتْ وَهُمْ
لَا يُظْلَمُونَ ﴿٢٨١﴾ ع ٣٨ ١

FUNGU 39

283. Enyi mlioamini, mnapokopeshana deni kwa muda uliowekwa, basi liandikeni. Na mwandishi aandike baina yenu kwa uadilifu, wala mwandishi asikatae kuandika kama Alivyomfunza Allah hivyo aandike.Na aandikishe (mkopi) ambaye juu yake iko haki, naye amwogope Allah, Mola wake, wala asipunguze cho chote ndani yake. Na kama yule ambaye juu yake iko haki ni mpumbavu

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا إِذَا تَدَايَنتُم بِدَيْنٍ إِلَىٰ
أَجَلٍ مُّسَمًّى فَاكْتُبُوهُ ۚ وَلْيَكْتُب بَّيْنَكُمْ
كَاتِبٌ بِالْعَدْلِ ۖ وَلَا يَأْبَ كَاتِبٌ أَن
يَكْتُبَ كَمَا عَلَّمَهُ اللَّهُ فَلْيَكْتُبْ ۚ
وَلْيُمْلِلِ الَّذِي عَلَيْهِ الْحَقُّ وَلْيَتَّقِ اللَّهَ رَبَّهُ
وَلَا يَبْخَسْ مِنْهُ شَيْئًا ۚ فَإِن كَانَ الَّذِي

Aya 283. Hizi hapa ni kanuni za deni. Kanuni hizi zimetangazwa na Qur'an miaka 1,400 iliyopita kabla dunia nzima haijaamka. Leo kila kuliko na ustaarabu kanuni hizi zinafuatwa.

Wanaume wenu, yaani mashahidi wawe watu wenu wanaokaa mahali mlipo, wasiwe wageni, ili wakitakiwa kutoa ushahidi watokee mara moja.

au mnyonge, au yeye hawezi kuandikisha mwenyewe, basi aandikishe wakili wake kwa adili. Na mshuhudishe mashahidi wawili katika wanaume wenu. Lakini ikiwa hakuna wanaume wawili, basi mwanamume mmoja na wanawake wawili katika wale mwapendao kuwa mashahidi, kama mmoja wao akisahau, mmoja wao amkumbushe mwingine. Na mashahidi wasikatae waitwapo. Wala msipuuze kuliandika, likiwa dogo au kubwa, mpaka muda wake: hayo ndiyo bora mbele ya Allah, na imara zaidi kwa ushahidi, na pia ni karibu ya kuwa msiwe na shaka, isipokuwa iwe biashara iliyohudhuria mnayopeana baina yenu, basi si dhambi kwenu msipoandika. Na shahidisheni mnapouziana. Wala asipate taabu mwandishi wala shahidi, na kama mkifanya hivyo, basi kwa hakika hilo ni kosa kwenu. Na mwogopeni Allah, na Allah ndiye Anayewaelimisheni; na Allah ni Mjuzi wa kila kitu.

عَلَيْهِ الْحَقُّ سَفِيْهًا اَوْ ضَعِيْفًا اَوْ لَا
يَسْتَطِيْعُ اَنْ يُّمِلَّ هُوَ فَلْيُمْلِلْ وَلِيُّهٗ
بِالْعَدْلِ ؕ وَاسْتَشْهِدُوْا شَهِيْدَيْنِ مِنْ
رِّجَالِكُمْ ۚ فَاِنْ لَّمْ يَكُوْنَا رَجُلَيْنِ
فَرَجُلٌ وَّامْرَاَتٰنِ مِمَّنْ تَرْضَوْنَ مِنَ
الشُّهَدَآءِ اَنْ تَضِلَّ اِحْدٰىهُمَا فَتُذَكِّرَ
اِحْدٰىهُمَا الْاُخْرٰى ؕ وَلَا يَاْبَ الشُّهَدَآءُ
اِذَا مَا دُعُوْا ؕ وَلَا تَسْـَٔمُوْٓا اَنْ تَكْتُبُوْهُ
صَغِيْرًا اَوْ كَبِيْرًا اِلٰٓى اَجَلِهٖ ؕ ذٰلِكُمْ اَقْسَطُ
عِنْدَ اللّٰهِ وَاَقْوَمُ لِلشَّهَادَةِ وَاَدْنٰٓى اَلَّا
تَرْتَابُوْٓا اِلَّآ اَنْ تَكُوْنَ تِجَارَةً حَاضِرَةً
تُدِيْرُوْنَهَا بَيْنَكُمْ فَلَيْسَ عَلَيْكُمْ جُنَاحٌ
اَلَّا تَكْتُبُوْهَا ؕ وَاَشْهِدُوْٓا اِذَا تَبَايَعْتُمْ ۪
وَلَا يُضَآرَّ كَاتِبٌ وَّلَا شَهِيْدٌ ؕ وَاِنْ تَفْعَلُوْا
فَاِنَّهٗ فُسُوْقٌۢ بِكُمْ ؕ وَاتَّقُوا اللّٰهَ ؕ
وَيُعَلِّمُكُمُ اللّٰهُ ؕ وَاللّٰهُ بِكُلِّ شَىْءٍ عَلِيْمٌ ﴿٢٨٢﴾

Mwapendao, yaani mashahidi hao wanaume au wanawake wawe ni watu wa maana ambao pande zote mbili zinawaamini.

Asipate taabu, yaani kama mwandishi kazi yake ni hiyo hiyo lazima alipwe ujira kwa kazi yake. Tena mashahidi na mwandishi wakiitwa mbele ya hakimu lazima walipwe gharama zao walizotumia kwa kuitika wito huo kama gharama za safari na nyinginezo.

Ni wazi kuwa kukopa deni hakukatazwi, maana kama mtu anakuwa katika taabu na shida anashurutishwa kukopa deni. Hapo sheria ya Kiislamu inasema, kwa mapatano mtu anaweza kukopa. Na Mtume *s.a.w.* amesema, "Kila deni ni sadaka" (Kashful-Ghummah). Lakini pia Mtume *s.a.w*. amesema, "Anayekopa deni na hana nia ya kurudisha, basi yeye ni mwizi," Na pia alikuwa anasema, "Mbora wenu ni ambaye ni mwema zaidi kwa kulipa deni" (Kashful-Ghummah).

Padre Dale ameandika mara kwa mara ya kuwa Mtume *s.a.w.* alichukua mafundisho ya Biblia akatunga nayo Qur'an. Tunamwuliza mafundisho hayo juu ya deni yaliyoelezwa katika fungu zima yameandikwa katika chuo gani cha Biblia? Au Kitabu gani kingine cha Sheria ya dini kina mafundisho kama hayo? Au Waarabu walikuwa na desturi hiyo katika siku za Mtume s.a.w.? Kama mtu asiyejua kuandika wala kusoma anaweza kutunga Kitabu kama Qur'an, kweli waungu watatu wa Ukristo ni duni kuliko mtu, maana hawakuweza kuteremsha mafundisho kama yake.

وَاِنْ كُنْتُمْ عَلٰى سَفَرٍ وَّلَمْ تَجِدُوْا كَاتِبًا
فَرِهٰنٌ مَّقْبُوْضَةٌ ؕ فَاِنْ اَمِنَ بَعْضُكُمْ
بَعْضًا فَلْيُؤَدِّ الَّذِى اؤْتُمِنَ اَمَانَتَهٗ وَلْيَتَّقِ
اللّٰهَ رَبَّهٗ ؕ وَلَا تَكْتُمُوا الشَّهَادَةَ ؕ وَمَنْ
يَّكْتُمْهَا فَاِنَّهٗۤ اٰثِمٌ قَلْبُهٗ ؕ وَاللّٰهُ بِمَا
تَعْمَلُوْنَ عَلِيْمٌ ﴿۲۸۳﴾ ع ۳۹/۷

284. Na kama mkiwa safarini na hamkupata mwandishi, basi rehani ikabidhiwe (mdai); lakini kama mmoja wenu ameweka amana kwa mwingine, basi aliyeaminiwa airudishe amana ya mwenzake, na amche Allah, Mola wake, Wala msifiche ushahidi; na atakayeuficha, basi hakika moyo wake ni wenye dhambi. Na Allah Huyajua mnayoyatenda.

FUNGU 40

لِلّٰهِ مَا فِى السَّمٰوٰتِ وَمَا فِى الْاَرْضِ ؕ وَاِنْ
تُبْدُوْا مَا فِىْۤ اَنْفُسِكُمْ اَوْ تُخْفُوْهُ
يُحَاسِبْكُمْ بِهِ اللّٰهُ ؕ فَيَغْفِرُ لِمَنْ يَّشَآءُ
وَيُعَذِّبُ مَنْ يَّشَآءُ ؕ وَاللّٰهُ عَلٰى كُلِّ شَىْءٍ
قَدِيْرٌ ﴿۲۸۴﴾

285. Vilivyomo mbinguni na vilivyomo ardhini ni vya Allah; na kama mkidhihirisha yaliyomo katika mioyo yenu, au mkiyaficha, Allah Atawatakeni hesabu ya hayo; basi Atamsamehe Amtakaye, na Atamwadhibu Amtakaye; na Allah ni Mwenye uwezo juu ya kila kitu.

اٰمَنَ الرَّسُوْلُ بِمَاۤ اُنْزِلَ اِلَيْهِ مِنْ رَّبِّهٖ
وَالْمُؤْمِنُوْنَ ؕ كُلٌّ اٰمَنَ بِاللّٰهِ وَمَلٰٓئِكَتِهٖ
وَكُتُبِهٖ وَرُسُلِهٖ ۫ لَا نُفَرِّقُ بَيْنَ اَحَدٍ مِّنْ
رُّسُلِهٖ ۫ وَقَالُوْا سَمِعْنَا وَاَطَعْنَا ۫
غُفْرَانَكَ رَبَّنَا وَاِلَيْكَ الْمَصِيْرُ ﴿۲۸۵﴾

286. Mtume ameamini yaliyoteremshwa kwake kutoka kwa Mola wake, na waaminio (pia): wote wamemwamini Allah, na Malaika Wake, na Vitabu Vyake, na Mitume Wake; (nao husema), hatutofautishi baina ya mmoja wa Mitume Wake; na husema, Tumesikia na tumetii. (Tunakuomba) msamaha, Mola wetu, na marudio ni kwako.

لَا يُكَلِّفُ اللّٰهُ نَفْسًا اِلَّا وُسْعَهَا ؕ لَهَا مَا
كَسَبَتْ وَعَلَيْهَا مَا اكْتَسَبَتْ ؕ رَبَّنَا لَا
تُؤَاخِذْنَاۤ اِنْ نَّسِيْنَاۤ اَوْ اَخْطَاْنَا ۚ رَبَّنَا وَلَا

287. Allah Haikalifishi nafsi yo yote ila yaliyo sawa na wasaa wake; (faida ya) yale iliyoyachuma ni yake na (hasara ya) yale iliyoyachuma

Aya 287. *Usitubebeshe mzigo.* Wakristo waliilaumu Sheria yao wakaisema ni laana. Hivyo rehema ya Mungu ikawa kwao mzigo na adhabu. Waislamu wanafundishwa kuomba ya kuwa

ni juu yake. Mola wetu, Usitushike kama tukisahau au tukikosa, Mola wetu, na Usitubebeshe mzigo kama Ulivyowabebesha wale waliokuwa kabla yetu. Mola wetu, Usitutwike tusiyoyaweza, na Utusamehe, na Utughofirie, na Uturehemu; Wewe ndiwe mlinzi wetu; basi Utusaidie juu ya watu makafiri.

تَحْمِلْ عَلَيْنَآ اِصْرًا كَمَا حَمَلْتَهٗ عَلَى
الَّذِيْنَ مِنْ قَبْلِنَا ۚ رَبَّنَا وَلَا تُحَمِّلْنَا مَا لَا
طَاقَةَ لَنَا بِهٖ ۚ وَاعْفُ عَنَّا ۟ وَاغْفِرْ لَنَا ۟
وَارْحَمْنَا ۟ اَنْتَ مَوْلٰىنَا فَانْصُرْنَا عَلَى
الْقَوْمِ الْكٰفِرِيْنَ ﴿۲۸۶﴾ ع

---

kwao Sheria iwe rehema siku zote.

Isr, "Mzigo," ni mzigo mzito unaomzuia mtu kwenda, yaani mzigo wa madhambi unaomfanya mtu asitende mema.

Wa'fu'annaa waghfir lanaa. "Na Utusamehe, na Utughofirie." Neno *'afw'* maana yake ni kufuta; na mradi wake ni kufuta au kusamehe madhambi (Mufradat); na *ghafr,* maana yake ni kufunika kwa kitu kinachohifadhi. Katika kitabu cha tafsiri ya Bukhari kiitwacho Sharha ya Kastalani, imeelezwa ya kwamba neno hili *ghafr* maana yake ni hifadhi ya namna mbili: (1) Kumhifadhi mtu asifanye dhambi na (2) kumhifadhi asipate adhabu ya dhambi aliyofanya. Katika Nihaya sifa ya Allah ya *Ghaafir* na *Ghafuur* zinasemwa maana yao ni "Anayestiri dhambi za watumishi wake na aibu zao, anayeacha hatia zao na dhambi zao."

Maneno haya mawili, *'awf* na *ghafr* yanatokea sana katika Qur'an. Na yanapokuwa yametumiwa pamoja namna hii, *'awf* linaleta maana ya kusamehe dhambi na mtu asipate adhabu, ilhali *ghafr* linaleta maana ya kulindwa ili mtu asiweze kutenda dhambi. Hivyo dua ya *Istighfaar* ni dua ya kuomba ili mtu asiwe na dhambi.

Habari hii inahusiana na watu wa zamani ambao walikabidhiwa madaraka ya kidini lakini wakayadharau madaraka hayo na wakayaona kuwa ni mzigo. Matokeo yake ni kwamba waalimu wa dini kutoka katika tabaka za chini za jamii wakabebeshwa mzigo ule mabegani mwao na hapo ndipo wakazaliwa viongozi wa dini ambao walihodhi elimu ya dini japokuwa hawakuwa na uwezo wa kuitumia kwa haki elimu hiyo. Mlolongo huu ndio hatimaye ukasababisha kutengenezwa kwa viongozi wa dini ambao walikuwa na akili finyu, wenye kiburi na wasiokuwa wavumilivu, na ni wachache miongoni mwao walioielewa falsafa na maadili ya neno la Mungu. Viongozi wa dini wa namna hiyo wamefananishwa na punda kaika Suuratul Jumu'ah aya ya 6 (62:6) ambao migongo yao imepakizwa shehena ya vitabu vya dini ili visafirishwe lakini hao punda wanaelewa kidogo tu kuhusu kile walichobeba. Kwa hiyo neno *Iswran* ni lazima lieleweke katika maana hii, kwa sababu wajibu wo wote uliowekwa na Allah hauwezi kuhesabiwa kuwa ni mzigo ambao waumini wa kweli wataomba kuepukana nao.

Katika Hadithi za Mtume *s.a.w.* dua hii ya mwisho wa sura hii imetukuzwa sana. Alisema, "Mtu atakayeomba kama ilivyofundishwa katika Aya mbili za mwisho za Surat-ul-Baqara, basi zinamtosha" (Bukhari). Tena imesimuliwa, "Mtume *s.a.w.* alipoomba kwa maombi haya, akaambiwa katika kila tamko, 'Imefanywa'." Na Mtume *s.a.w.* akasema. "Allah ameteremsha Aya hizi mbili toka hazina za Peponi." (Baidhawi).

سُوْرَةُ اٰلِ عِمْرٰنَ مَدَنِيَّةٌ وَّ هِيَ مَعَ الْبَسْمَلَةِ مِائَتَا اٰيَةٍ وَّ اٰيَةٌ وَّ عِشْرُوْنَ رُكُوْعًا

3. SURA AALI 'IMRAAN

Imeteremshwa Madina

Ina mafungu 20 na Aya 201 pamoja na Bismillah

بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ ①

1. Kwa jina la Allah, Mwingi wa rehema, Mwingi wa ukarimu.

الٓمّٓ ②

2. Mimi ni Allah Nijuaye sana.

اللّٰهُ لَآ اِلٰهَ اِلَّا هُوَ ۙ الْحَيُّ الْقَيُّوْمُ ③

3. Allah hakuna aabudiwaye isipokuwa Yeye, Mzima wa milele, Mhifadhi wa milele.

نَزَّلَ عَلَيْكَ الْكِتٰبَ بِالْحَقِّ مُصَدِّقًا لِّمَا بَيْنَ يَدَيْهِ وَاَنْزَلَ التَّوْرٰىةَ وَالْاِنْجِيْلَ ۙ ④

4. Amekuteremshia Kitabu kwa haki kinachosadikisha yaliyokuwa kabla yake; na Aliteremsha Taurati na Injili

مِنْ قَبْلُ هُدًى لِّلنَّاسِ وَاَنْزَلَ الْفُرْقَانَ ؕ اِنَّ الَّذِيْنَ كَفَرُوْا بِاٰيٰتِ اللّٰهِ لَهُمْ عَذَابٌ شَدِيْدٌ ؕ وَاللّٰهُ عَزِيْزٌ ذُو انْتِقَامٍ ⑤

5. hapo kabla, kuwa mwongozo kwa watu; na Ameteremsha Kipambanuzi. Hakika wale waliozikufuru aya za Allah wana adhabu kali; na Allah ni Mwenye ushindi kamili, Mwenye kisasi.

Sura hii ina majina mengi katika Hadithi. Nayo pia inaitwa *Az-Zahraa* (Ing'aayo). Pia inaitwa *Al-Amaan* (Amani), *Al-Kanz* (Hazina), *Al-Mu'iina* (Msaidizi), *Al-Mujaadala* (Utetezi), *Al-Istighfaar* (Kuomba Ghofira), na *Tayyiba* (Safi). Imeitwa *Aali 'Imraan* kwa sababu ya habari ya watoto wa Imraani waliotajwa katika Aya ya 34.

Aya 3. Aya hii inavunja kwa nguvu uungu wa Yesu, ambayo ndiyo habari kubwa inayoelezwa katika sura hii. Sura hii imeanza na sifa za Allah zinazokata kabisa mzizi wa fundisho hilo la Ukristo. (1) "Mzima wa milele" na "Mhifadhi wa milele" ni sifa ambazo mwenye nazo hawezi kuwa na haja ya msaidizi. Yesu aliyetawaliwa na kanuni ya kuzaliwa na kufa hangeweza kuwa mzima wa milele na mhifadhi wa milele, na hivyo hawezi kuwa Mungu.

Aya 4. *Kwa haki:* yaani. (1) Qur'an ina mafundisho yaliyo sahihi na ambayo ye yote hawezi kufanikiwa akitaka kuyashambulia; (2) Qur'an imeteremshwa wakati sawasawa, yaani walioipokea mwanzoni walikuwa ndiyo watu waliostahili kabisa kuipokea; (3) Imekuja katika wakati inapohitajiwa, na kufika kwake kumetimiza haja iliyokuwepo; (4) Imekuja kaa moja kwa moja na hata maadui zake wajitahidi namna gani hawawezi kufanikiwa kuiangamiza au kuivuruga.

Kinachosadikisha: Neno Muswaddiqan lina matumizi mapana. Lina maana ya kusadikisha ukweli wa funuo zilizotangulia na pia kutimiliza na kuziweka bayana tabiri zilizomo katika funuo hizo.

Al-Furqaan: Ina maana ya ukweli usiokanika na vilevile kitu chenye kupambanua waziwazi kitu kimoja katika kingine; kwa hiyo kinafanya kazi kama kigezo.

إِنَّ اللّٰهَ لَا يَخْفٰى عَلَيْهِ شَيْءٌ فِي الْأَرْضِ وَلَا فِي السَّمَآءِ ۝٦

6. Bila shaka Allah kwake hakifichiki cho chote kilichomo ardhini wala kilichomo mbinguni.

هُوَ الَّذِيْ يُصَوِّرُكُمْ فِي الْأَرْحَامِ كَيْفَ يَشَآءُ ۚ لَآ إِلٰهَ إِلَّا هُوَ الْعَزِيْزُ الْحَكِيْمُ ۝٧

7. Yeye ndiye Huwatengenezeni sura matumboni jinsi Apendavyo; hakuna aabudiwaye ila Yeye, Mwenye nguvu, Mwenye hekima.

هُوَ الَّذِيْٓ أَنْزَلَ عَلَيْكَ الْكِتٰبَ مِنْهُ اٰيٰتٌ مُّحْكَمٰتٌ هُنَّ أُمُّ الْكِتٰبِ وَأُخَرُ مُتَشٰبِهٰتٌ ۚ فَأَمَّا الَّذِيْنَ فِيْ قُلُوْبِهِمْ زَيْغٌ فَيَتَّبِعُوْنَ مَا تَشَابَهَ مِنْهُ ابْتِغَآءَ الْفِتْنَةِ وَابْتِغَآءَ تَأْوِيْلِهٖ ۗ وَمَا يَعْلَمُ تَأْوِيْلَهٗٓ إِلَّا اللّٰهُ ۘ وَالرّٰسِخُوْنَ فِي الْعِلْمِ يَقُوْلُوْنَ اٰمَنَّا بِهٖ ۙ كُلٌّ مِّنْ عِنْدِ رَبِّنَا ۚ وَمَا يَذَّكَّرُ إِلَّآ أُولُوا الْأَلْبَابِ ۝٨

8. Yeye ndiye Aliyekuteremshia Kitabu, ndani yake zimo Aya Muhkam, zilizo asili ya Kitabu; na zingine Mutashaabihaat. Lakini wale ambao mioyoni mwao mna upotofu, basi wanafuata zinazofanana kwa kuitaka fitina na kutamani maelezo yake (wayatakayo); na hakuna ajuaye tafsiri yake ila Allah, na wale waliozama katika elimu, husema: Tumeziamini, zote zimetoka kwa Mola wetu; na hawazingatii nasaha isipokuwa wenye akili.

رَبَّنَا لَا تُزِغْ قُلُوْبَنَا بَعْدَ إِذْ هَدَيْتَنَا وَهَبْ لَنَا مِنْ لَّدُنْكَ رَحْمَةً ۚ إِنَّكَ أَنْتَ الْوَهَّابُ ۝٩

9. Mola wetu, Usiipotoshe mioyo yetu baada ya kutuongoza, na Utupe rehema kutoka Kwako, hakika Wewe ndiwe Mpaji Mkuu.

Aya 8. *Muhkam.* Neno hili mradi wake ni (1) iliyohifadhika isiyoweza kubadilika au kugeuka; (2) isiyo na maana zingine-zingine au kuweza kufanyiwa shaka; (3) iliyo na maana ya wazi (Akrab na Mufradat).

Mutashaabihaat mradi wake ni (1) maneno au Aya ambayo inaweza kuwa na tafsiri mbalimbali ingawa zinazowafikiana; (2) ile ambayo sehemu zake zinafanana au zinapatana na Aya au maneno mengine; (3) ile ambayo mradi wake wa hasa unafanana na maana isiyokusudiwa; au (4) ile ambayo maana yake ya kweli haijulikani ila kwa kuipambanisha na Aya *muhkam;* (5) ile ambayo haiwezi kufahamiwa barabara bila kufikiriwa mara kwa mara.

Ambao mioyoni mwao mna upotofu. Maneno hayo yanaeleza kanuni inayofaa sana. Watu watawa wanaotaka kufahamu hakika inayokusudiwa na Aya inayoweza kuwa na maana mbili au zaidi hujaribu kuleta maelezo yanayofanana na Aya iliyo *muhkam.* Ama wale ambao mna upotofu mioyoni mwao, huipa Aya hiyo maana iliyo kinyume cha Aya hizo za asili.

Wakristo wangeshika kanuni hii wasingeunda miungu mingine kinyume cha amri ya Allah. Umoja wa Mungu ni jambo ambalo limetiwa mkazo katika Biblia. Lakini Wakristo wameacha mafundisho hayo yote na wakapendelea *Mutashaabihaat* ambazo ni Aya zenye maneno kama "Mwana wa Mungu" ambazo zingefaa zifasiriwe kwa kuweka mbele aya zilizo *muhkam,* kama hizi: "Usiwe na waungu wengine mbele zangu" (Kutoka 20:2, 3; Kumbukumbu 5:7, Hosea 13:4). "Sikiza ewe Israeli: Jehova Allah wetu, Jehova ni mmoja" (Kumbukumbu 6:4, 5). Yesu alipoulizwa alijibu. "Katika amri zote amri ya kwanza ni hii, Sikiliza Israeli, Rabbi Mungu wako ni Mungu mmoja" (Marko 12:29).

رَبَّنَآ اِنَّكَ جَامِعُ النَّاسِ لِيَوْمٍ لَّا رَيْبَ فِيْهِ ؕ اِنَّ اللّٰهَ لَا يُخْلِفُ الْمِيْعَادَ ۝٩ ع

10. Mola wetu, Kwa yakini Wewe ndiwe Mkusanyaji wa watu katika Siku isiyo na shaka ndani yake. Hakika Allah Havunji miadi.

FUNGU 2

اِنَّ الَّذِيْنَ كَفَرُوْا لَنْ تُغْنِيَ عَنْهُمْ اَمْوَالُهُمْ وَلَآ اَوْلَادُهُمْ مِّنَ اللّٰهِ شَيْـًٔا ؕ وَاُولٰٓئِكَ هُمْ وَقُوْدُ النَّارِ ۝١١

11. Kwa hakika wale waliokufuru, mali zao hazitawafaa wala watoto wao hata kidogo kwa Allah, na hao ndiyo kuni za Moto.

كَدَاْبِ اٰلِ فِرْعَوْنَ ۙ وَالَّذِيْنَ مِنْ قَبْلِهِمْ ؕ كَذَّبُوْا بِاٰيٰتِنَا ۚ فَاَخَذَهُمُ اللّٰهُ بِذُنُوْبِهِمْ ؕ وَاللّٰهُ شَدِيْدُ الْعِقَابِ ۝١٢

12. Sawa na mwenendo wa watu wa Firauni na wale waliokuwa kabla yao, walikadhibisha Aya Zetu, kwa hiyo Allah Akawashika kwa sababu ya madhambi yao; na Allah ni mkali wa kuadhibu.

قُلْ لِّلَّذِيْنَ كَفَرُوْا سَتُغْلَبُوْنَ وَتُحْشَرُوْنَ اِلٰى جَهَنَّمَ ؕ وَبِئْسَ الْمِهَادُ ۝١٣

13. Waambie wale waliokufuru: Karibuni mtashindwa na mtakusanywa kwenye Jahanamu, nacho ni kikao kibaya.

قَدْ كَانَ لَكُمْ اٰيَةٌ فِيْ فِئَتَيْنِ الْتَقَتَا ؕ فِئَةٌ تُقَاتِلُ فِيْ سَبِيْلِ اللّٰهِ وَاُخْرٰى كَافِرَةٌ

14. Hakika ilikuwa Ishara kwa ajili yenu katika makundi mawili yaliyokutana; kundi moja lilipigana katika njia ya Allah, na

---

Aya 13. *Karibuni ninyi mtashindwa.* Kutimia bishara anazotabiri Nabii ni njia mojawapo ya kuhakikisha ukweli wake. Mtume *s.a.w.* anaambiwa kuwapasha Waarabu wa Makka na Mayahudi wa Madina wasiosilimu habari ya kushindwa kwao. Katika siku zile Mtume s.a.w. alikuwa amezungukwa na maadui, Waarabu na Mayahudi, waliokuwa shauri moja katika kuuangamiza Uislamu. Mtu vivi hivi hangeweza kusema habari kama ile kisha ikatimia. Hakika hiyo ilikuwa elimu ya Allah iliyomwezesha Mtume kusema hayo mbele, na ilikuwa nguvu ya Mweza wa yote iliyovunja heshima ya maadui.

Mtakusanywa kwenye Jahanamu. Qur'an ilitabiri mambo mawili: (1) Kushindwa maadui na (2) kukusanywa kwao kwenye Jahanamu. Kwa kuunga pamoja mambo ya dunia na ya Akhera, Mungu anataka kuonyesha ya kuwa likitimia linaloonekana, itakuwa ni dalili ya kwamba hata lile lisiloonekana pia litatimia. Na kwa kuwa kushindwa na maadui wa Uislamu kulitimia, basi kukusanywa kwao Motoni pia kutatimia.

Aya 14. *Makundi mawili.* Ni majeshi mawili yaliyopigana katika mtaa wa Badri, karibu na Madina. Kundi dogo la Waislamu 313, wasio na silaha za maana wala zana, lilipolishinda jeshi la makafiri lililokuwa na askari hodari 1,000 wenye ustadi na zana na silaha barabara. Hapa zilitimia bishara mbili, moja iliyoelezwa katika Biblia (Isaya 21:13-17), na nyingine ndani ya Qur'an (sura 54:45-49).

يَّرَوْنَهُمْ مِّثْلَيْهِمْ رَاْىَ الْعَيْنِ ؕ وَاللّٰهُ
يُؤَيِّدُ بِنَصْرِهٖ مَنْ يَّشَآءُ ؕ اِنَّ فِيْ ذٰلِكَ
لَعِبْرَةً لِّاُولِي الْاَبْصَارِ ﴿١٤﴾

jingine makafiri, wakawaona zaidi kuliko wao mara mbili kwa kuona kwa macho; na Allah Humwauni kwa nusura yake Amtakaye; kwa yakini katika hayo limo onyo kwa wenye busara.

زُيِّنَ لِلنَّاسِ حُبُّ الشَّهَوٰتِ مِنَ النِّسَآءِ
وَالْبَنِيْنَ وَالْقَنَاطِيْرِ الْمُقَنْطَرَةِ مِنَ
الذَّهَبِ وَالْفِضَّةِ وَالْخَيْلِ الْمُسَوَّمَةِ
وَالْاَنْعَامِ وَالْحَرْثِ ؕ ذٰلِكَ مَتَاعُ الْحَيٰوةِ
الدُّنْيَا ۚ وَاللّٰهُ عِنْدَهٗ حُسْنُ الْمَاٰبِ ﴿١٥﴾

15. Watu wamepambiwa huba ya matamanio ya wanawake na watoto na marundo ya dhahabu na fedha, na farasi wanaotunzwa, na wanyama na mashamba; hayo ni matumizi ya maisha ya dunia; na kwa Allah ndiko kwenye marudio mazuri.

قُلْ اَؤُنَبِّئُكُمْ بِخَيْرٍ مِّنْ ذٰلِكُمْ ؕ لِلَّذِيْنَ
اتَّقَوْا عِنْدَ رَبِّهِمْ جَنّٰتٌ تَجْرِيْ مِنْ
تَحْتِهَا الْاَنْهٰرُ خٰلِدِيْنَ فِيْهَا وَاَزْوَاجٌ
مُّطَهَّرَةٌ وَّرِضْوَانٌ مِّنَ اللّٰهِ ؕ وَاللّٰهُ بَصِيْرٌۢ
بِالْعِبَادِ ﴿١٦﴾ ۚ

16. Sema: Je, niwaambieni yaliyo bora kuliko hayo? Kwa ajili ya wamchao Allah ziko Bustani kwa Mola wao, ambazo ndani yake hupita mito; watakaa humo milele, humo pia wako wenzi waliotakaswa na Allah na pia imo radhi ya Allah; Na Allah ni Mwenye kufahamu vyema kuhusu waja Wake:

اَلَّذِيْنَ يَقُوْلُوْنَ رَبَّنَاۤ اِنَّنَاۤ اٰمَنَّا فَاغْفِرْ لَنَا
ذُنُوْبَنَا وَقِنَا عَذَابَ النَّارِ ﴿١٧﴾ ۚ

17. (Hizo ni kwa ajili ya wale) wasemao: Mola wetu, hakika sisi tumeamini, basi Utughofirie madhambi yetu, na Utuepushe na adhabu ya Moto;

اَلصّٰبِرِيْنَ وَالصّٰدِقِيْنَ وَالْقٰنِتِيْنَ
وَالْمُنْفِقِيْنَ وَالْمُسْتَغْفِرِيْنَ بِالْاَسْحَارِ ﴿١٨﴾

18. Wafanyao subira, na wasemao kweli, na watii, na watoao (katika njia ya Allah), na waombao ghofira kabla ya alfajiri.

شَهِدَ اللّٰهُ اَنَّهٗ لَاۤ اِلٰهَ اِلَّا هُوَ ۙ وَالْمَلٰٓئِكَةُ
وَاُولُوا الْعِلْمِ قَآئِمًۢا بِالْقِسْطِ ؕ لَاۤ اِلٰهَ اِلَّا
هُوَ الْعَزِيْزُ الْحَكِيْمُ ﴿١٩﴾

19. Allah Anashuhudia Akisimama kwenye uadilifu kwamba hakuna mwabudiwa isipokuwa Yeye tu na Malaika na wale wenye elimu nao pia wanashuhudia vivyo hivyo; Hakuna mwabudiwa isipokuwa Yeye tu, Mwenye uwezo kamili, Mwenye hekima.

Aya 19: Kwa hakika maneno ya Kiarabu *Qaaiman bilqistwi* yana maana iliyo nzito zaidi kuliko ile ya msimamizi wa haki inayoonyeshwa na tafsiri hapo juu. Tafsiri nzuri zaidi ni hii: 'Akiwa amesimama daima kuilinda haki'.

20. Bila shaka dini hasa mbele ya Allah ni Islamu; na waliopewa Kitabu hawakuhitilafiana ila baada ya kuwajia elimu, kwa sababu ya uasi uliokuwa kati yao; na anayezikataa Aya za Allah, basi hakika Allah ni Mwepesi wa kuhesabu.

إِنَّ الدِّيْنَ عِنْدَ اللّٰهِ الْإِسْلَامُ ۗ وَمَا
اخْتَلَفَ الَّذِيْنَ اُوْتُوا الْكِتٰبَ اِلَّا مِنْۢ بَعْدِ
مَا جَآءَهُمُ الْعِلْمُ بَغْيًۢا بَيْنَهُمْ ۗ وَمَنْ
يَّكْفُرْ بِاٰيٰتِ اللّٰهِ فَاِنَّ اللّٰهَ سَرِيْعُ الْحِسَابِ ۝١٩

21. Na kama wakikuhoji basi useme: Nimejitupa kwa Allah, na pia walionifuata; na waambie wale waliopewa Kitabu na wasio na elimu: Je, mmesilimu? Basi kama wakisilimu bila shaka wameongoka; na kama wakikengeuka; basi juu yako ni kufikisha tu; Na Allah Huwaona sana watumishi.

فَاِنْ حَآجُّوْكَ فَقُلْ اَسْلَمْتُ وَجْهِيَ لِلّٰهِ
وَمَنِ اتَّبَعَنِ ۗ وَقُلْ لِّلَّذِيْنَ اُوْتُوا الْكِتٰبَ
وَالْاُمِّيّٖنَ ءَاَسْلَمْتُمْ ۗ فَاِنْ اَسْلَمُوْا فَقَدِ
اهْتَدَوْا ۚ وَاِنْ تَوَلَّوْا فَاِنَّمَا عَلَيْكَ الْبَلٰغُ ۗ
وَاللّٰهُ بَصِيْرٌۢ بِالْعِبَادِ ۝٢٠ ع ٢

FUNGU 3

22. Hakika wale wanaozikataa Aya za Allah, na kuwapinga Manabii pasipo haki, na kuwapinga watu wanaoamuru mambo ya uadilifu, basi wapashe habari za adhabu iumizayo.

اِنَّ الَّذِيْنَ يَكْفُرُوْنَ بِاٰيٰتِ اللّٰهِ وَيَقْتُلُوْنَ
النَّبِيّٖنَ بِغَيْرِ حَقٍّ ۙ وَّيَقْتُلُوْنَ الَّذِيْنَ
يَاْمُرُوْنَ بِالْقِسْطِ مِنَ النَّاسِ ۙ فَبَشِّرْهُمْ
بِعَذَابٍ اَلِيْمٍ ۝٢١

23. Hao ndiyo vitendo vyao vimeharibika katika dunia na Akhera nao hawatapata wasaidizi.

اُولٰٓئِكَ الَّذِيْنَ حَبِطَتْ اَعْمَالُهُمْ فِي الدُّنْيَا
وَالْاٰخِرَةِ ۖ وَمَا لَهُمْ مِّنْ نّٰصِرِيْنَ ۝٢٢

24. Je, huwaoni wale waliopewa sehemu ya Kitabu, wanaitwa kwenye Kitabu cha Allah ili Awahukumu baina yao, kisha kundi moja miongoni mwao hukengeuka, nao wamekwenda upande.

اَلَمْ تَرَ اِلَى الَّذِيْنَ اُوْتُوْا نَصِيْبًا مِّنَ
الْكِتٰبِ يُدْعَوْنَ اِلٰى كِتٰبِ اللّٰهِ لِيَحْكُمَ
بَيْنَهُمْ ثُمَّ يَتَوَلّٰى فَرِيْقٌ مِّنْهُمْ وَهُمْ
مُّعْرِضُوْنَ ۝٢٣

Aya 24. *Sehemu ya Kitabu,* yaani: (1) Sehemu ya Biblia yenye bishara zinazomhusu Mtume Muhammad *s.a.w.*; (2) Sehemu halisi ya Biblia iliyobaki salama bila kuharibiwa; (3) kwa kulinganisha na Kitabu bora cha Qur'an, Biblia inakuwa ni sehamu tu.

Kitabu cha Allah, yaani, Qur'an. Mayahudi wanaitwa kuhukumiwa na Qur'an; na si kama adhanivyo Padre Dale ya kuwa wanatakiwa kuhukumiwa na Biblia. Padre anauliza,

ذٰلِكَ بِاَنَّهُمْ قَالُوْا لَنْ تَمَسَّنَا النَّارُ اِلَّآ اَيَّامًا مَّعْدُوْدٰتٍ ۖ وَغَرَّهُمْ فِيْ دِيْنِهِمْ مَّا كَانُوْا يَفْتَرُوْنَ ﴿٢٥﴾

25. Hayo ni kwa sababu walisema: Hautatugusa Moto isipokuwa kwa siku chache; na yakawadanganya katika dini yao yale waliyokuwa wakiyatunga.

فَكَيْفَ اِذَا جَمَعْنٰهُمْ لِيَوْمٍ لَّا رَيْبَ فِيْهِ ۗ وَوُفِّيَتْ كُلُّ نَفْسٍ مَّا كَسَبَتْ وَهُمْ لَا يُظْلَمُوْنَ ﴿٢٦﴾

26. Basi itakuwaje tutakapowakusanya Siku ambayo haina shaka ndani yake; na kila nafsi itapewa sawasawa iliyoyachuma, nao hawatadhulumiwa.

قُلِ اللّٰهُمَّ مٰلِكَ الْمُلْكِ تُؤْتِي الْمُلْكَ مَنْ تَشَآءُ وَتَنْزِعُ الْمُلْكَ مِمَّنْ تَشَآءُ ۖ وَتُعِزُّ مَنْ تَشَآءُ وَتُذِلُّ مَنْ تَشَآءُ ۭ بِيَدِكَ الْخَيْرُ ۭ اِنَّكَ عَلٰي كُلِّ شَيْءٍ قَدِيْرٌ ﴿٢٧﴾

27. Sema: Ee Mola, Mmiliki wa Ufalme! Humpa ufalme Umtakaye, na Humwondolea ufalme Umtakaye, na Humwenzi Umtakaye, na Kumdhalilisha Umtakaye; heri imo mkononi Mwako. Bila shaka Wewe ni Mwenye uwezo juu ya kila kitu.

تُوْلِجُ الَّيْلَ فِي النَّهَارِ وَتُوْلِجُ النَّهَارَ فِي الَّيْلِ ۡ وَتُخْرِجُ الْحَيَّ مِنَ الْمَيِّتِ وَتُخْرِجُ الْمَيِّتَ مِنَ الْحَيِّ ۡ وَتَرْزُقُ مَنْ تَشَآءُ بِغَيْرِ حِسَابٍ ﴿٢٨﴾

28. Wewe Huingiza usiku katika mchana, na Huingiza mchana katika usiku, na Hutoa aliye hai katika yule asiye na uhai, na hutoa mfu katika yule aliye hai; na Humruzuku Umtakaye bila hesabu.

"Kitabu kisicho sahihi chawezaje kuhukumu?" Swali hili labda kidogo lingeonekana lenye kufaa kama mradi wa Kitabu cha Mungu hapa ungekuwa ni Biblia. Lakini si Biblia bali wanaitwa kwenye Qur'an.

Kadhalika kama tulivyokwisha onyesha. Taurati kuitwa "sehemu ya Kitabu" si jambo la kumshangaza Padre Dale, maana siyo mradi wake ya kwamba Taurati waliyonayo ni kamili bali ni sehemu tu. Ndani yake imo sehemu iliyobaki salama bila kuharibika, kama bishara za kufika Mtume *s.a.w.* na habari zake zingine zinazokubaliwa na Qur'an.

Aya 26. *Itapewa sawasawa iliyoyachuma.* Aya hii ni kinyume kabisa na fundisho la dini ya Kikristo lisemalo kuwa si matendo ya mwenye nayo ila ni damu ya Yesu iliyo kafara ya kuondoa dhambi za watu.

Aya 27 na 28. Aya hizi zinaeleza kuwa taifa la Waisraeli lililokuwa na ufalme wa kidunia na kidini na uhai wa kiroho sasa litanyang'anywa yote hayo na watapewa taifa jingine la Waislamu sawa na agano alilopata Nabii Ibrahimu kwa Allah ya kuwa *ahadi yangu haitawafikia wadhalimu* (sura 2:125).

لَا يَتَّخِذِ الْمُؤْمِنُوْنَ الْكٰفِرِيْنَ اَوْلِيَآءَ
مِنْ دُوْنِ الْمُؤْمِنِيْنَ ۚ وَمَنْ يَّفْعَلْ ذٰلِكَ
فَلَيْسَ مِنَ اللّٰهِ فِيْ شَيْءٍ اِلَّآ اَنْ تَتَّقُوْا
مِنْهُمْ تُقٰىةً ؕ وَيُحَذِّرُكُمُ اللّٰهُ نَفْسَهٗ ؕ
وَاِلَى اللّٰهِ الْمَصِيْرُ ﴿٢٩﴾

29. Waaminio wasiwafanye makafiri kuwa marafiki badala ya waaminio; na atakayefanya hivyo, basi hatakuwa na cho chote kwa Allah, isipokuwa ya kwamba mjilinde nao kabisa; na Allah Anawahadharisheni na nafsi Yake; na marudio ni kwa Allah.

قُلْ اِنْ تُخْفُوْا مَا فِيْ صُدُوْرِكُمْ اَوْ تُبْدُوْهُ
يَعْلَمْهُ اللّٰهُ ؕ وَيَعْلَمُ مَا فِي السَّمٰوٰتِ وَمَا
فِي الْاَرْضِ ؕ وَاللّٰهُ عَلٰى كُلِّ شَيْءٍ قَدِيْرٌ ﴿٣٠﴾

30. Sema: Kama mkificha yaliyomo vifuani mwenu au kuyadhihirisha, Allah Atayajua; na Anayajua yaliyomo mbinguni, na yaliyomo ardhini; na Allah ni Mwenye uwezo juu ya kila kitu.

يَوْمَ تَجِدُ كُلُّ نَفْسٍ مَّا عَمِلَتْ مِنْ خَيْرٍ
مُّحْضَرًا ۚ وَّمَا عَمِلَتْ مِنْ سُوْٓءٍ ۚ تَوَدُّ
لَوْ اَنَّ بَيْنَهَا وَبَيْنَهٗٓ اَمَدًا بَعِيْدًا ؕ
وَيُحَذِّرُكُمُ اللّٰهُ نَفْسَهٗ ؕ وَاللّٰهُ رَءُوْفٌ
بِالْعِبَادِ ﴿٣١﴾ ع ١١

31. Siku ambayo kila nafsi itakuta mema iliyoyafanya yamehudhurishwa, na pia ubaya ilioufanya. Itapenda lau kungekuwa na nafasi kubwa baina yake na baina (ya ubaya); na Allah Anawatahadharisheni na nafsi Yake, na Allah ni Mpole kwa watumishi.

FUNGU 4

قُلْ اِنْ كُنْتُمْ تُحِبُّوْنَ اللّٰهَ فَاتَّبِعُوْنِيْ
يُحْبِبْكُمُ اللّٰهُ وَيَغْفِرْ لَكُمْ ذُنُوْبَكُمْ ؕ
وَاللّٰهُ غَفُوْرٌ رَّحِيْمٌ ﴿٣٢﴾

32. Sema: Ikiwa ninyi mwampenda Allah, basi nifuateni, Allah Atawapendeni na Atawaghofirieni madhambi yenu; na Allah ni Mwenye ghofira, Mwenye rehema.

قُلْ اَطِيْعُوا اللّٰهَ وَالرَّسُوْلَ ۚ فَاِنْ تَوَلَّوْا
فَاِنَّ اللّٰهَ لَا يُحِبُّ الْكٰفِرِيْنَ ﴿٣٣﴾

33. Sema: Mtiini Allah na Mtume, na kama wakikengeuka, basi Allah Hawapendi Makafiri.

Aya 29. *Anawatahadharisheni na nafsi Yake.* maneno ya Kiarabu *Yuhadh-dhirukumulaahu nafsahu* kwa tafsiri ya neno kwa neno yana maana kwamba 'Mwenyezi Mungu anawatahadharisheni dhidi ya Yeye Mwenyewe', ambayo inamaanisha kwamba anawatahadharisheni msifanye mtakavyo kuhusu amri na maonyo yake. Maneno hayo pia yanaweza kutafsiriwa hivi *Anawatahadharisheni na adhabu Yake,* maana neno *nafsi* pia linaweza kuwa na maana ya *adhabu* (Akrab na Lane).

34. Hakika Allah Alimchagua Adamu na Nuhu na watoto wa Ibrahimu na watoto wa Imrani juu ya walimwengu.

35. Wazao, wao kwa wao; na Allah ni Mwenye kusikia, Mwenye kujua.

36. (Kumbukeni) aliposema mwanamke wa Imrani: Mola wangu, hakika nimeweka nadhiri Kwako aliyomo tumboni mwangu kuwa wakfu; basi nikubalie. Bila shaka Wewe ndiwe Usikiaye, Ujuaye.

37. Basi alipomzaa akasema: Mola wangu, hakika nimemzaa mwanamke - na Allah Anajua sana aliyemzaa - na mwanamume si kama mwanamke - na bila shaka nimempa jina Mariamu, nami hakika namkinga Kwako, yeye na wazao wake, Uwalinde na shetani arujumiwaye.

إِنَّ اللّٰهَ اصْطَفٰٓى اٰدَمَ وَنُوْحًا وَّ اٰلَ
اِبْرٰهِيْمَ وَاٰلَ عِمْرٰنَ عَلَى الْعٰلَمِيْنَ ﴿٣٤﴾
ذُرِّيَّةًۢ بَعْضُهَا مِنْۢ بَعْضٍ ؕ وَ اللّٰهُ
سَمِيْعٌ عَلِيْمٌ ﴿٣٥﴾
اِذْ قَالَتِ امْرَاَتُ عِمْرٰنَ رَبِّ اِنِّيْ
نَذَرْتُ لَكَ مَا فِيْ بَطْنِيْ مُحَرَّرًا فَتَقَبَّلْ
مِنِّيْ ۚ اِنَّكَ اَنْتَ السَّمِيْعُ الْعَلِيْمُ ﴿٣٦﴾
فَلَمَّا وَضَعَتْهَا قَالَتْ رَبِّ اِنِّيْ وَضَعْتُهَآ
اُنْثٰى ؕ وَاللّٰهُ اَعْلَمُ بِمَا وَضَعَتْ ؕ وَلَيْسَ
الذَّكَرُ كَالْاُنْثٰى ۚ وَاِنِّيْ سَمَّيْتُهَا مَرْيَمَ
وَاِنِّيْٓ اُعِيْذُهَا بِكَ وَذُرِّيَّتَهَا مِنَ الشَّيْطٰنِ
الرَّجِيْمِ ﴿٣٧﴾

Aya 34. *Imrani,* Jina hili huenda liwe kwa ajili ya watu wawili: (1) Amram, anayetajwa katika Biblia, aliyekuwa mwana wa Kohath na aliyekuwa mjukuu wa Lawi. Yeye alikuwa baba wa Musa, Harun na Miriam (Jewish Encyclopaedia; Kutoka 6:18-20); (2) Imran, baba wa Mariamu mamaye Yesu. Huyu Imran alikuwa mwana wa Yoshhim au Yoshim (Jarir na Kathir).

Aya 36. *Mwanamke wa Imrani.* Mwanamke anayetajwa hapa ni mama wa Mariamu. Kumwita *mwanamke wa Imrani* ni kifupisho cha kumwita *mwanamke wa ukoo wa Imrani.* (2) Kadhalika *mwanamke wa Imrani* inaweza kuwa "mke wa Imrani" ambaye jina lake aliitwa Hana (Enc. Bib). Kwa hakika kuna habari hasa inayoeleza kuwa mume wa Hana ambaye ni baba wa Mariamu aliitwa Imrani Bin Yoshhim au Yoshim (Jarir na Kathir). Hivyo Imrani huyu ni mbali na Imrani yule aliyekuwa baba wa Musa ambaye aliitwa Imran Bin Kohath (Kutoka 6: 18-20).

Aya 37. *Nimempa jina Mariamu.* Alimpa jina la dada ya Musa na Harun. Na kwa kuwa Mariamu alitolewa wakfu akae ujane katika hekalu, na kwa kuwa kazi za mahekalu zilikuwa mikononi mwa makuhani, Harun na wazao wake, basi Qur'an ikampanga jina "Dada wa Harun" (sura 19:20) kwa vile ameingia katika ukuhani ambayo ni kazi ya Nabii Harun.

Rajiim. Neno hili maana yake: (1) Ambaye Mungu Amemfukuza mbele Yake na katika rehema Yake; (2) aliyelaaniwa na Mungu; (3) aliyeachwa, na (4) aliyepigwa mawe (Akrab na Lane). Pia maana yake ni ambaye amefukuziliwa mbali na kunyimwa wema wote (Mufradat).

فَتَقَبَّلَهَا رَبُّهَا بِقَبُوْلٍ حَسَنٍ وَّاَنْۢبَتَهَا نَبَاتًا
حَسَنًا ۙ وَّكَفَّلَهَا زَكَرِيَّا ؕ كُلَّمَا دَخَلَ عَلَيْهَا
زَكَرِيَّا الْمِحْرَابَ ۙ وَجَدَ عِنْدَهَا رِزْقًا ۚ
قَالَ يٰمَرْيَمُ اَنّٰى لَكِ هٰذَا ؕ قَالَتْ هُوَ مِنْ
عِنْدِ اللّٰهِ ؕ اِنَّ اللّٰهَ يَرْزُقُ مَنْ يَّشَآءُ
بِغَيْرِ حِسَابٍ ﴿۳۸﴾

38. Basi Mola wake Akamkubali (yule mtoto) kwa ukubali mwema, na Akamlea kwa ulezi mwema, na akamfanya Zakaria awe mlinzi wake. Kila mara Zakaria alipoingia chumbani kwake alikuta riziki pamoja naye. Akasema: Ewe Mariamu, unapata wapi hii? Akasema: Hii hutoka kwa Allah; hakika Allah Humruzuku Amtakaye bila hesabu.

هُنَالِكَ دَعَا زَكَرِيَّا رَبَّهٗ ۚ قَالَ رَبِّ هَبْ
لِيْ مِنْ لَّدُنْكَ ذُرِّيَّةً طَيِّبَةً ۚ اِنَّكَ
سَمِيْعُ الدُّعَآءِ ﴿۳۹﴾

39. Pale pale Zakaria akamwomba Mola wake, akasema: Mola wangu, Unipe kutoka Kwako wazao wazuri; kwa yakini Wewe ndiwe Usikiaye maombi.

فَنَادَتْهُ الْمَلٰٓئِكَةُ وَهُوَ قَآئِمٌ يُّصَلِّيْ فِي
الْمِحْرَابِ ۙ اَنَّ اللّٰهَ يُبَشِّرُكَ بِيَحْيٰى
مُصَدِّقًا بِكَلِمَةٍ مِّنَ اللّٰهِ وَسَيِّدًا وَّحَصُوْرًا
وَّنَبِيًّا مِّنَ الصّٰلِحِيْنَ ﴿۴۰﴾

40. Mara Malaika wakamnadia hali amesimama akisali chumbani ya kwamba Allah Anakupa habari njema ya Yahya, atakayekuwa mwenye kusadikisha neno adhimu litokalo kwa Allah, na atakayekuwa Seyyidi na mtawa na Nabii miongoni mwa watu wema.

قَالَ رَبِّ اَنّٰى يَكُوْنُ لِيْ غُلٰمٌ وَّقَدْ بَلَغَنِيَ
الْكِبَرُ وَامْرَاَتِيْ عَاقِرٌ ؕ قَالَ كَذٰلِكَ اللّٰهُ
يَفْعَلُ مَا يَشَآءُ ﴿۴۱﴾

41. Akasema: Mola wangu, nitapataje mtoto na hali uzee umenifikia na mke wangu ni tasa! Akasema: Hivyo ndivyo Allah Hufanya Apendavyo.

قَالَ رَبِّ اجْعَلْ لِّيْۤ اٰيَةً ؕ قَالَ اٰيَتُكَ اَلَّا
تُكَلِّمَ النَّاسَ ثَلٰثَةَ اَيَّامٍ اِلَّا رَمْزًا ؕ
وَاذْكُرْ رَّبَّكَ كَثِيْرًا وَّسَبِّحْ بِالْعَشِيِّ
وَالْاِبْكَارِ ﴿۴۲﴾ ع ۱۳

42. Akasema: Mola wangu, Uniwekee alama. Akasema, Alama yako ni kutosema na watu kwa siku tatu isipokuwa kwa ishara tu; na umtaje Mola wako kwa wingi na umtukuze wakati wa jioni na asubuhi.

FUNGU 5

وَاِذْ قَالَتِ الْمَلٰٓئِكَةُ يٰمَرْيَمُ اِنَّ اللّٰهَ
اصْطَفٰىكِ وَطَهَّرَكِ وَاصْطَفٰىكِ عَلٰى
نِسَآءِ الْعٰلَمِيْنَ ﴿۴۳﴾

43. Na (kumbukeni) Malaika waliposema: Ewe Mariamu, kwa hakika Allah Amekuchagua na kukutakasa na kukutukuza kuliko wanawake wa walimwengu.

يٰمَرْيَمُ اقْنُتِيْ لِرَبِّكِ وَاسْجُدِيْ وَارْكَعِيْ مَعَ الرّٰكِعِيْنَ ﴿٤٣﴾

44. Ewe Mariamu, umnyenyekee Mola wako na usujudu na uiname pamoja na wainamao.

ذٰلِكَ مِنْ اَنْۢبَآءِ الْغَيْبِ نُوْحِيْهِ اِلَيْكَ ؕ وَمَا كُنْتَ لَدَيْهِمْ اِذْ يُلْقُوْنَ اَقْلَامَهُمْ اَيُّهُمْ يَكْفُلُ مَرْيَمَ ۪ وَمَا كُنْتَ لَدَيْهِمْ اِذْ يَخْتَصِمُوْنَ ﴿٤٤﴾

45. Hizo ni katika habari za ghaibu Tunazokufunulia; nawe hukuwa nao walipokuwa wakitupa mishale yao (kwa kura wajue) nani wao atamwangalia Mariamu, na hukuwa nao walipokuwa wakibishana.

اِذْ قَالَتِ الْمَلٰٓئِكَةُ يٰمَرْيَمُ اِنَّ اللّٰهَ يُبَشِّرُكِ بِكَلِمَةٍ مِّنْهُ ۖ اسْمُهُ الْمَسِيْحُ عِيْسَى ابْنُ مَرْيَمَ وَجِيْهًا فِي الدُّنْيَا وَالْاٰخِرَةِ وَمِنَ الْمُقَرَّبِيْنَ ﴿٤٥﴾

46. (Kumbukeni) waliposema Malaika: Ewe Mariamu, bila shaka Allah Anakupa habari njema za neno litokalo Kwake, jina lake Masihi Isa mwana wa Mariamu, mwenye heshima katika dunia na Akhera, na yu miongoni mwa walio karibu (na Allah).

وَيُكَلِّمُ النَّاسَ فِي الْمَهْدِ وَكَهْلًا وَّمِنَ الصّٰلِحِيْنَ ﴿٤٦﴾

47. Naye atazungumza na watu katika utoto na katika utu uzima, na atakuwa miongoni mwa watu wema.

Aya 45. *Aqlaamahum,* "Mishale yao." Neno hilo kwa Kiarabu ni: (1) Tete linalotumiwa kwa kuandika linapokwisha chongwa kama kalamu; (2) mshale usio na ncha unaotumiwa kwa kupigia kura; (3) mshale au kikuki kidogo (Akrab).

Aya 46. *Neno litokalo Kwake.* Mapadre wanasema kwa kuwa Qur'an inasema Yesu ni neno lililotoka kwa Mungu, ati inakubali Yesu ni mtoto wa Mungu. Dhana hii ni kutapatapa kwa bure. Stadi mkubwa wa lugha ya Kiarabu aliyetunga *Taaj-ul-Aruus* anasema ya kuwa Yesu ameitwa *Kalimatullaah* kwa sababu maneno yake yalisaidia kazi ya dini. Kama vile mtu anayesaidia dini kwa ushujaa wake anaitwa *Saifullaah* (Upanga wa Mungu) au *Asadullaah* (Simba wa Mungu), hivyo ndivyo tamko la *kalimatullaah.*

Neno Kalima limetumiwa katika Qur'an kwa ajili ya vitu vingi. Kwa mfano Allah Amesema, "Sema, kama bahari ingalikuwa wino kwa kuyaandika maneno (kalimaat) ya Mola wangu bila shaka bahari ingalikwisha kabla ya kwisha kalimaat (maneno) ya Mola wangu, na ingawa Tungalileta bahari kama hiyo kuongezea" (sura 18: 110). Kama kwa kalima maelezo ya mapadre ya kusema Yesu ni mwana wa Mungu yakubaliwe, je, vitu vyote na viumbe vyote vilivyoitwa kalimaatullaah vitakuwa wana wa Mungu?

Tena ikiwa Yesu aneitwa kalima (neno), Mtume s.a.w. ameitwa Dhikr yaani Kitabu au hotuba nzuri (sura 65:11, 12) ambayo ni dhahiri ina kalima nyingi.

Aya 47. *Naye atazungumza.* Siyo maana yake kujisemea tu maneno bali maana yake ni kuwa atazungumza mambo ya busara na hekima. Kadhalika ilivyosemwa, katika utoto na katika utu uzima ilibashiriwa kuwa Nabii Isa hatakufa katika utoto bali atakuwa hai hata utu uzima; naye alipokufa alikuwa na umri wa miaka 120 (Mawaahibulladunniyya, Jalada 1 uk. 42). Yesu kusema maneno ya busara bali angali mtoto hakuna kioja cho chote ndani yake. Watoto wengi

48. (Mariamu) akasema: Mola wangu, nitampataje mtoto na hali mtu ye yote hajanigusa? Akasema: Hivyo ndivyo Allah Huumba Anavyopenda; Anapohukumu jambo basi Huliambia tu, kuwa, basi huwa.

قَالَتْ رَبِّ اَنّٰى يَكُوْنُ لِىْ وَلَدٌ وَّلَمْ يَمْسَسْنِىْ بَشَرٌ ؕ قَالَ كَذٰلِكِ اللّٰهُ يَخْلُقُ مَا يَشَآءُ ؕ اِذَا قَضٰٓى اَمْرًا فَاِنَّمَا يَقُوْلُ لَهٗ كُنْ فَيَكُوْنُ ﴿۴۸﴾

49. Na (Allah) Atamfunza Kitabu na hekima na Taurati na Injili.

وَيُعَلِّمُهُ الْكِتٰبَ وَالْحِكْمَةَ وَالتَّوْرٰىةَ وَالْاِنْجِيْلَ ﴿۴۹﴾

50. Naye atakuwa Mtume wa kuwafikishia wana wa Israeli ujumbe huu kwamba, Nimewajieni na Ishara kutoka kwa Mola wenu, ya kwamba nitawaumbieni kama ndege watengenezavyo, kisha nitapulizia ndani yake, mara atakuwa ndege (wa kiroho) kwa idhini ya Allah. Na nitamponya kipofu na mwenye ukoma, na kuwahuisha wafu (wa kiroho) kwa idhini ya Allah, na ninawaambieni mtakavyovila na mtakavyoweka akiba katika nyumba zenu; bila shaka katika hayo imo ishara kwenu ikiwa ninyi mnaamini.

وَرَسُوْلًا اِلٰى بَنِىْٓ اِسْرَآءِيْلَ ۙ اَنِّىْ قَدْ جِئْتُكُمْ بِاٰيَةٍ مِّنْ رَّبِّكُمْ ۙ اَنِّىْٓ اَخْلُقُ لَكُمْ مِّنَ الطِّيْنِ كَهَيْـَٔةِ الطَّيْرِ فَاَنْفُخُ فِيْهِ فَيَكُوْنُ طَيْرًا بِاِذْنِ اللّٰهِ ۚ وَاُبْرِئُ الْاَكْمَهَ وَالْاَبْرَصَ وَاُحْىِ الْمَوْتٰى بِاِذْنِ اللّٰهِ ۚ وَاُنَبِّئُكُمْ بِمَا تَاْكُلُوْنَ وَمَا تَدَّخِرُوْنَ ۙ فِىْ بُيُوْتِكُمْ ؕ اِنَّ فِىْ ذٰلِكَ لَاٰيَةً لَّكُمْ اِنْ كُنْتُمْ مُّؤْمِنِيْنَ ۚ ﴿۵۰﴾

---

wenye akili na waliolelewa vizuri huzungumza namna hiyo.

Neno la "Mahdi" tumelitafsiri hapa "utoto," kwa kufuata mradi wake. Neno lenyewe maana yake ni "Kitanda cha mtoto."

Aya 48. *Anapohukumu jambo basi Huliambia tu, kuwa, basi huwa:* Maneno *'kuwa basi huwa'* hayaonyeshi mageuzi kutoka katika hali ya kutokuwepo na kujileta yenyewe katika hali ya kuwepo pasipo kutendeshwa. Maneno hayo yana maana kwamba mara tu Allah Anapokusudia jambo, basi kusudio lake hilo huanza kuumbika na hatimae linafanyika kama Alivyokusudia.

Aya 49. Neno *Kitaab* (Kitabu) linatoa maana mbili: "Kitabu" na "Ujuzi wa kuandika." Kama neno hili hapa litachukuliwa kwa maana ya 'Kitabu' basi mradi wake utakuwa ni 'Taurati', Sheria ya Musa, na hivyo maneno yanayomaliza. "Taurati na Injili" yatafahamiwa kuwa maelezo yake, neno 'Taurat' likisimamia 'Kitabu' na neno 'Injili' likisimamia hekima.

Aya 50. *Mtume kwa wana wa Israeli.* Aya hii inadhihirisha ya kuwa Yesu hakuwa Mjumbe kwa ajili ya ulimwengu wote, bali kwa ajili ya wana wa Israeli tu.

Injili inaeleza waziwazi kusudi la kufika kwa Yesu. Si shauri la wafuasi wake kuteua wafanye nini na wasifanye nini katika kueneza dini yake. Mungu Mwenyewe Aliyemtuma Yesu ndiye Anajua Alimtuma afanye kazi namna gani. Na Yesu aliyetumwa ndiye anayejua ni maagizo gani aliyopewa na Allah juu ya kazi ya kuhubiri dini. Yesu mwenyewe amesema, "Sikutumwa ila kwa kondoo waliopotea wa nyumba ya Israeli" (Matt. 15:24); "Kwa maana mwana

wa Adamu alikuja kukiokoa kilichopotea" (Matt. 18:11).

Hivyo mafundisho ya Yesu ni kwa ajili ya Waisraeli tu. Inasemwa ya kwamba Yesu alisema, "Basi enendeni, mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza kwa jina la Baba na Mwana, na Roho Mtakatifu" (Matt. 28:19). Lakini kuhoji kuwa kwa aya hii Yesu aliwaamuru wanafunzi wake wakahubirie watu wote si sawa. Maana yake ni hii tu ya kuwa aliwaamuru kwa maneno hayo waende kwa *makabila yote ya Israeli,* siyo kwa mataifa yote. Yesu anasema kwa maneno yaliyo wazi: "Amini, nawaaambia ya kwamba ninyi mlionifuata mimi, katika ulimwengu mpya atakapoketi mwana wa Adamu katika kiti cha utukufu wake, ninyi nanyi mtaketi katika viti kumi na viwili, mkiwahukumu kabila kumi na mbili za Israeli" (Matt. 19:28). "Sikutumwa ila kwa kondoo waliopotea wa nyumba ya Israeli" (Matt. 15:24). "Msiwape mbwa kilicho kitakatifu, wala msitupe lulu zenu mbele ya nguruwe" (Matt. 7:6). Mwanamke mmoja asiyekuwa Myahudi alimwomba Yesu amrehemu: Yesu alijibu, "Si vema kukitwaa chakula cha watoto na kuwatupia mbwa" (Matt. 15:26). Majibu haya yanaonyesha kwamba mbwa au nguruwe ni watu wasiokuwa Waisraeli.

WANAFUNZI WALITUMWA KWA MAYAHUDI TU

Tena tunasoma, "Hao thenashara Yesu aliwatuma, akawaagiza akisema, katika njia ya mataifa msiende, wala katika mji wo wote wa Wasamaria msiingie. Afadhali shikeni njia kuwaendea kondoo waliopotea wa nyumba ya Israeli" (Matt. 10:5-6). Mtu asidhani ya kuwa linaloagizwa hapa ni ya kwamba wahubiri wa Kikristo kwanza waende miji ya Waisraeli na kisha kwa watu wengine. La, si hivyo, maana kuwaendea kondoo waliopotea wa nyumba ya Israeli siyo maana yake kuitembelea tu miji yao, bali kuwaingiza Ukristo. Hivyo linaloagizwa hapa ni kwamba wasiende kamwe kwa watu wengine mpaka Waisraeli wote watakapokwisha ingia Ukristo. Yesu amebainisha ya kuwa, kazi ya kuwahubiria Waisraeli na kuwaingiza katika Ukristo haitakwisha mpaka kufika kwake mara ya pili. Anasema, "Lakini watakapowafukuza katika mji huu, kimbilieni mwingine; maana ni kweli nawaambia, hamtaimaliza miji ya Israeli, hata ajapo mwana wa Adamu" (Matt. 10:23).

Katika hayo ni wazi ya kwamba Mathayo 28:19 inawataka wahubiri wa Kikristo wasimamishe Ukristo katika miji ya Waisraeli na siyo kuitembelea tu. Inaonyeshwa wazi ya kuwa kazi hii ya kuwahubiria Waisraeli haitakwisha mpaka Yesu kuja tena. Kwa hiyo Mapadre kwenda hubiria watu wengine kabla Yesu hajaja, ni kufanya mambo kinyume kabisa na mafundisho ya Yesu.

Isitoshe, kuambiwa kwenda hubiria mataifa yote, lisimdanganye mtu kudhania mataifa yote ya dunia, kama tulivyokwisha bainisha. Maneno kama haya yametumika katika Injili kwa kuonyesha watu maalumu tu. Kwa mfano Luka (2:1) anasema, "Siku zile amri ilitoka kwa Kaisari Augosto ya kwamba iandikwe orodha ya majina ya *watu wote wa ulimwengu.*" Ni wazi ya kwamba Kaisari hakumiliki ulimwengu mzima, na hangeweza kuhesabu majina ya watu wote wa ulimwengu. Hivyo ingawa imeandikwa "watu wote wa ulimwengu," makusudi yake ni watu wote waliokuwa katika milki yake. Hivyo, hata kama Yesu aseme waende kwa "mataifa yote," maana yake itakuwa ni mataifa ya Waisraeli, yaani makabila yao yote.

Tena imeandikwa katika Matendo 15:21, "Tangu zamani za kale Musa anao watu wahubirio mambo yake; katika kila mji husomwa kila sabato katika masinagogi," Je, kwa maneno haya tunaweza kusema Musa alikuwa na watu wanaohubiri katika kila mji duniani? La, Bali ingawa imeandikwa "kila mji" mradi wake ni miji ya Waisraeli tu, siyo kila mji duniani. Hivyo kama Yesu alisema wanafunzi wake waendee mataifa yote, mradi wake ni mataifa yote ya Waisraeli, yaani makabila yao.

Tena Matendo 24:5 imeandikwa, "Kwa maana tumemwona mtu huyu mkorofi, mwanzilizi wa fitina katika Mayahudi wote duniani." Ni wazi kabisa ya kuwa ingawa Paulo anasemwa hapa ni mwanzilizi wa fitina katika, "Mayahudi wote duniani," yeye hakuwahi kufika sehemu zingine za dunia zilizokuwa na Mayahudi, kama bara Hindi (Esitheri 1 na 2). Hivyo Yesu kusema, waende kwa mataifa yote, kwa uandishi wa Injili, siyo maana yake ila ni kuwaendea mataifa ya Mayahudi tu.

WANAFUNZI WALIHUBIRIA MAYAHUDI

Wanafunzi wa Yesu pia wanaona sivyo kwenda kuwahubiria wasiokuwa Waisraeli. Tunasoma, "Basi wale waliotawanyika kwa sababu ya ile dhiki iliyotukia kwa habari ya Stefano, wakasafiri hata Foinike na Kipro na Antiokia, wasilihubiri lile neno ila kwa Mayahudi peke yao" (Matendo 11:19).

Kadhalika wanafunzi wa Yesu waliposikia kuwa Petro, mahali fulani amewahubiria wasiokuwa Waisraeli, walikasirika: "Na Petro alipopanda kwenda Yerusalemu, wale walio na tohara wakashindana naye, wakisema, Uliingia kwa watu wasiotahiriwa ukalala nao" (Matendo 11:2-3). Na jinsi alivyojibu Petro haonyeshi kuwa kulikuwa ruhusa ya Yesu kwenda kuhubiria mataifa mengine; bali anasema tu ya kwamba aliona ndotoni ale kila namna ya mnyama aliyoko duniani na ya kwamba Roho alimwambia aende huko. Hakusema aliambiwa na Yesu. Na kwa kuwa Paulo anaeleza ya kuwa Petro alikuwa na unafiki (Wagalatia 2:11), tunaona mashaka kabisa kukubali ndoto hizi za kula ovyo hata vitu vilivyoharimishwa na Mungu (Walawi 11), na kwenda hubiria waliokatazwa na Yesu mbele ya watu wote.

SABABU ZA PAULO KUYAENDEA MATAIFA

Ama sababu iliyomfanya Paulo kwenda huburia wasio Mayahudi, ni kwamba Mayahudi fulani walimpinza wasitake kumkubalia. Imeandikwa, "Hata Sila na Timotheo walipotelemka kutoka Makedonia. Paulo akashurutishwa rohoni mwake akiwashuhudia Wayahudi ya kwamba Yesu ni Kristo. Walipopingamana naye na kutukana, akakung'uta mavazi yake , akiwaambia, Damu yenu na iwe juu ya vichwa vyenu; mimi ni safi; tangu sasa nitakwenda kwa watu wa mataifa" (Matendo 18:5-6).

Paulo alikata shauri hivi, labda kwa vile hakuwa mwanafunzi wa Yesu toka mwanzo, na pengine hakusikia agizo la Bwana alilosema waziwazi, "Katika njia ya mataifa msiende, wala katika mji wo wote wa Wasamaria msiingie. Afadhali shikeni njia kuwaendea kondoo waliopotea wa nyumba ya Israeli" (Matt. 10:5-6).

Toka hapo Paulo alianza kuhubiri kwa wasio Mayahudi pia, akitaka kupata watu wengi, kama asemavyo mwenyewe, "Nalijifanya mtumwa wa wote ili nipate watu wengi zaidi" (1 Wakor 9:19). Na ingawa Paulo anamshitaki Petro kuwa alikuwa na unafiki (Wagalatia 2:11), tunaona ya kwamba naye alijitokeza kwa watu kwa njia isiyomfaa mtu mkweli wa dini. Yeye mwenyewe anasema, "Nalikuwa kama Myahudi kwa Wayahudi, ili niwapate Wayahudi; kwa wale walio chini ya sheria, nalikuwa kama chini ya sheria, ili niwapate walio chini ya sheria. Kwa wale wasio na sheria nalikuwa kama sina sheria . . . . ili niwapate hao wasio na sheria." (Wakor 9:20-21).

Mtu aliye na hali kama hii anayojisifu nayo Bwana Paulo, kila mtu avute mawazo yake kidogo tu kupimia alikuwa akifanya nini kilicho mradi wa hayo maneno yake. Je, ni kama hivi ya kwamba Padre Mkatoliki afikapo kwa Waislamu aanze kusali Kiislamu, aache kula nguruwe, na afunge Ramadhani, ili Waislamu wamdhanie ni mwenzao ili apate kuwavuta? Na afikapo kwa Waprotestanti aanze kumsifu Martin Luther na kujidai hasujudii masanamu, na afikapo kwa wamizimu, naye pia aanze kutambika ili awapate watambikaji na waprotestanti? Je, hiyo ni njia inayofaa kwa kuhubiri dini?

Siku moja Bwana Paulo akamtahiri Myunani mmoja ili kuwafanya Mayahudi wasitambue kuwa si mmoja wao na kumlaumu. Imeandikwa, "Basi akafika Derbe na Listra, na hapo palikuwa na mwanafunzi mmoja jina lake Timotheo, mwana wa mwanamke Myahudi aliyeamini; lakini babaye alikuwa Myunani. Mtu huyo alishuhudiwa vema na ndugu waliokaa Listra na Ikonio. Paulo akamtaka huyo afuatane naye, akamtwaa akamtahiri kwa ajili ya Mayahudi waliokuwa pande zile, kwa maana wote walijua ya kuwa babaye ni Myunani" (Matendo 116:1-3). Je, ni uaminifu huo?

UTATANISHI KATIKA NDOTO YA PAULO

Na kama tujuavyo, Bwana Paulo hakuwa mwanafunzi wa Yesu. Yeye anasema aliingia Ukristo kwa kuona ndoto alipokuwa akienda Damishki kuwakamata wafuasi wa Yesu. Katika ndoto hiyo anasema, alimwona Yesu akimkemea kwa sababu yeye Paulo aliwatia udhia Wakristo. Ndoto hiyo imeandikwa katika sura 9, 22 na 26 za kitabu cha Matendo. Na kama utaisoma, jinsi maelezo ya upande mmoja yanavyopingana na maelezo ya upande mwingine, hungependa mtu akuambie kuwa ndoto hiyo ilikuwa ya kweli.

1. Katika 9:3-6 imeandikwa, "Ghafla ikamwangaza kote kote nuru kutoka mbinguni. Akaanguka chini, akasikia sauti ikimwambia, Sauli, Sauli, ... Na wale watu waliosafiri pamoja naye wakasimama kimya, wakisikia sauti, wasione mtu." Lakini katika 22:9, anasema "Na wale waliokuwa pamoja nami waliiona ile nuru, lakini hawakusikia ile sauti ya yule aliyesema nami."

2. Katika 9:36 na 22:6-10 anasema, nuru kubwa ilimfunika yeye. Lakini katika sura 26:6-10 anasema, nuru ilimfunika yeye na wale waliofuatana naye.

3. Katika sura ya 9 tunasoma ya kuwa ni yeye tu aliyeanguka chini, na wengine wakasimama kimya; lakini katika sura 26:14, anasema ya kwamba yeye pamoja na waliofuatana naye wote wakaanguka chini.

4. Katika sura 22:10 anasema, alipouliza afanye nini, Yesu akamwambia, "Simama, uingie Dameski, na huko utaambiwa habari za mambo yote yaliyoamriwa ufanye." Alipofika Dameski mtu mmoj aitwaye Anania akamjia akamwambia yanayompasa kufanya. Lakini katika sura 26 haelezi hayo, bali anasema Yesu mwenyewe ndiye alimwambia mambo yote yaliyompasa kufanya.

Sasa mtu anayetumwa kwa ushahidi unaopandana kama huu, ambao kupingana kwake ni sababu za kutosha kuukataa kuwa si wa kweli, aje na avunje kabisa kanuni iliyowekwa na Yesu mwenyewe. mbele ya wanafunzi wake wote ya kuwa dini yake isihubiriwe isipokuwa kwa Mayahudi peke yao. Je, tuache ushahidi wa wanafunzi wake kumi na wawili wateule, tufuate maneno ya mtu aliyekuwa adui yake mkubwa na ambaye ndoto anayosema aliiona anatapatapa kuieleza sawasawa? Je ndoto kama hiyo inasadikika? Hamwoni Paulo mwenyewe amekwisha jifichua na kutueleza hakika ya habari zake zote kwa kusema. "Ikiwa kweli ya Mungu imezidi kwa sababu ya uwongo wangu hata akapata utukufu, mbona mimi nami ningali nikihukumiwa kama ni mwenye dhambi?" (Warumi 3:7). Nasi ndivyo tulivyokuwa tukishuku uwongo kusaidia kweli ya Mungu!

KURANI IMESEMA KWELI

Hivyo, ni wazi ya kwamba Wakristo hawana sababu za haki kwa kwenda kuhubiria dini watu ambao si Mayahudi. Na maneno yaliyosemwa na Qur'an kuwa Yesu alitumwa kwa wana wa Israeli tu yanashuhudiwa hata na maneno ya Yesu mwenyewe aliposema, "Sikutumwa ila kwa kondoo waliopotea wa nyumba ya Israeli" (Matt. 15:24).

Nawaumbieni katika udongo sawa na matengenezo ya ndege, kisha napulizia ndani yake, mara huwa ndege. Hapa ustadi wa Nabii Isa wa kusema maneno kwa mifano unadhihirika vizuri. Kwanza anawafananisha wanafunzi wake na udongo - yaani watu wanyonge walio duni. Kisha kwa mafundisho yake anawatengeneza mara wanakuwa kama wafu waliotiwa roho zenye nguvu: na badala ya kutembea ardhini maisha ya kidunia, wanakuwa kama ndege wapaao mbinguni katika maisha safi ya kimbingu.

Mafundisho haya ya Nabii Isa yamewatatiza wengi hata wakafika kudhani ya kwamba haikosi alikuwa akiumba ndege, na hali wanasahau ya kuwa sifa ya kuumba ni makhtasi kwa ajili ya Allah tu, na ya kuwa hata hakuna kiumbe cho chote kilichoshiriki sifa hii ingawa kwa uchache. Someni: sura 13:17; 16:21; 22:74; 25:4; 31:11-12; 35:41 na 46:5.

Na ninamponya kipofu na mwenye ukoma, na kuwahuisha wafu. Kama Mjuavyo Manabii ni Madaktari wakubwa wa roho. Kazi yao ni ngumu. Kumponya ambaye macho ya roho yake yamepofuka, na aliyeenewa na ukoma wa roho, ni kazi ngumu kupita kiasi. Na wanaofanikiwa

وَمُصَدِّقًا لِّمَا بَيْنَ يَدَيَّ مِنَ التَّوْرٰىةِ
وَلِأُحِلَّ لَكُمْ بَعْضَ الَّذِيْ حُرِّمَ عَلَيْكُمْ
وَجِئْتُكُمْ بِاٰيَةٍ مِّنْ رَّبِّكُمْ ۖ فَاتَّقُوا اللّٰهَ
وَاَطِيْعُوْنِ ﴿٥١﴾

51. Na msadikishaji wa yale yaliyokuwa kabla yangu katika Taurati, na ili niwahalalishieni baadhi ya yale mliyoharamishiwa, na nimewajieni na Ishara (kubwa) kutoka kwa Mola wenu, kwa hiyo Mcheni Allah na nitiini.

اِنَّ اللّٰهَ رَبِّيْ وَرَبُّكُمْ فَاعْبُدُوْهُ ۗ هٰذَا
صِرَاطٌ مُّسْتَقِيْمٌ ﴿٥٢﴾

52. Hakika Allah ni Mola wangu na ni Mola wenu, basi Mwabuduni; hii ndiyo njia iliyonyooka.

فَلَمَّآ اَحَسَّ عِيْسٰى مِنْهُمُ الْكُفْرَ قَالَ مَنْ
اَنْصَارِيْٓ اِلَى اللّٰهِ ۗ قَالَ الْحَوَارِيُّوْنَ
نَحْنُ اَنْصَارُ اللّٰهِ ۚ اٰمَنَّا بِاللّٰهِ ۚ وَاشْهَدْ بِاَنَّا
مُسْلِمُوْنَ ﴿٥٣﴾

53. Lakini Isa alipohisi (mwelekeo wa) kukataa kwao, akasema: Nani watakuwa wasaidizi wangu katika kuita kwenye njia ya Allah? Wanafunzi wakasema: Sisi ni wasaidizi wa Allah , na ushuhudie ya kwamba sisi ndiyo wajisalimishao.

رَبَّنَآ اٰمَنَّا بِمَآ اَنْزَلْتَ وَاتَّبَعْنَا الرَّسُوْلَ
فَاكْتُبْنَا مَعَ الشّٰهِدِيْنَ ﴿٥٤﴾

54. Mola wetu, tumeyaamini Uliyoyateremsha, na tumemfuata Mtume, basi Utuandike pamoja na watoao ushahidi wa haki.

---

kuitenda, bila shaka wametoka kwa Allah. Hapa Nabii Isa anataka kuwaambia watu wanaomkataa, Je, hamwoni watu waliokuwa wabaya sana sasa wamekuwa wacha-Mungu kwa kunifuata? Hii kwa hakika ni kazi ya kila Nabii wa kweli, kuwatakasa vipofu na wakoma wa kiroho.

Bila shaka mtaona ya kuwa magonjwa hayo yaliyoponywa ni ya kiroho ambayo huwa yanawafisha watu. Hata hivyo Manabii wa Allah wanawahuisha wafu hao wa kiroho pia, wakawa wazima wamchao Mungu. Allah amesema. "Enyi mlioamini, Mwitikieni Allah na Mtume anapowaiteni kwenye yale yatakayowapeni uhai" (sura 8:25). Basi hivi ndivyo Manabii hufufua wafu. Siyo maana yake wanafufua watu waliotoka roho kabisa. Aya za Qur'an zinazokataa kufufuka kwa namna hiyo ni hizi: Sura 23:100-101; 21:96; 39:59-60; 2:29; 49:12; 45:12; 45:27. Pia hadithi za Mtume *s.a.w.* zimeeleza jambo hili waziwazi kuwa wafu waliotoka roho hawarudi duniani. Kwa mfano inasimuliwa ya kuwa baba wa Jabir aliuwawa katika vita vya Uhud, na mwanawe huyu alihuzunika sana. Mtume *s.a.w.* akamtuliza na akamwambia. Allah alimwambia baba yako kwa mapenzi sana amwombe cho chote atakacho na atapewa. Basi babaye Jabir akaomba. "Mola wangu nipe muda mwingine wa kuishi duniani ili nikauawe tena katika njia Yako," Allah akamjibu. "Bila shaka ningekufanyia hivyo, lakini kauli yangu imekwisha tangulia kutoka ya kwamba wafu hawatarejeshwa duniani" (Tirmidhi na Ibni

Niwahalalishieni baadhi ya yale mliyoharimishiwa. Nabii Isa hakutangua sehemu yo yote ya Taurati; bali tu aliwahalalishia Mayahudi vitu ambavyo walikuwa wakihitilafiana wao kwa wao; na ambavyo wanazuoni waliviharimisha baada ya Musa (Kathir, Muhit).

وَمَكَرُوْا وَمَكَرَ اللّٰهُ ؕ وَاللّٰهُ خَيْرُ الْمٰكِرِيْنَ ﴿۵۵﴾

55. Na (wapinzani wa Masihi) walifanya mpango, na Allah Naye Akafanya mpango, Na Allah ni Mbora wa wafanyao mipango.

FUNGU 6

اِذْ قَالَ اللّٰهُ يٰعِيْسٰۤى اِنِّىْ مُتَوَفِّيْكَ وَرَافِعُكَ اِلَىَّ وَمُطَهِّرُكَ مِنَ الَّذِيْنَ كَفَرُوْا وَجَاعِلُ الَّذِيْنَ اتَّبَعُوْكَ فَوْقَ الَّذِيْنَ كَفَرُوْۤا اِلٰى يَوْمِ الْقِيٰمَةِ ۚ ثُمَّ اِلَىَّ مَرْجِعُكُمْ فَاَحْكُمُ بَيْنَكُمْ فِيْمَا كُنْتُمْ فِيْهِ تَخْتَلِفُوْنَ ﴿۵۶﴾

56. (Kumbukeni) Allah Aliposema: Ewe Isa, kwa yakini Mimi Ndiye mwenye kukufisha na kukuinua kwangu, na Nitakutakasa na (masingizio ya) wale waliokufuru, na Nitawaweka wale waliokufuata juu ya wale waliokufuru mpaka siku ya Kiyama; kisha marudio yenu ni Kwangu, ndipo Nitawahukumuni katika yale mliyokuwa mkihitilafiana.

Aya 55. *Makr.* "Hila," au "mpango" Neno hili lina maana mbili: (1) *Makr Mahmuud,* yaani hila au mpango mzuri ya kutaka kupatia jambo zuri, na *Makr madhmuum,* yaani hila au mpango mbaya wa kutaka kupatia kitu kibaya (Mufradat). Mayahudi walifanya hila ya kutaka kumfisha Nabii Isa a.s. kifo cha *laana* cha msalaba, lakini Allah Alipanga ya kuwa aokoke. Mpango wa Mayahudi ukapinduliwa na mpango wa Allah ukashinda, Nabii Isa asife msalabani akateremshwa hali ya kuzimia. Na baadaye akazindukana akaenda kufa kifo cha kawaida, hali yu mtu mzima mwenye miaka mingi, huko Kashmir. Pia tazama 4:158.

Aya 56. *Mutawaffiika,* "Nitakufisha." Ibni Abbas. nduguye Mtume *s.a.w.* na ambaye alikuwa mwanachuoni mkubwa kabisa, ametafsiri *Mutawaffiika* kuwa *Mumiituka* yaani, Nitakufisha (Bukhari). Kadhalika Zamakhshari, mwanachuoni wa lugha ya Kiarabu mwenye kusifika sana, amesema: "Tamko la Mutawaffiika maana yake, Nitakulinda usiuwawe na watu na Nitakupa muda kamili wa uhai uliowekwa kwa ajili yako na *Nitakufisha kifo cha ajali,* siyo cha kuuawa" (Kashshaf). Kwa hakika wanachuoni wote wa lugha ya Kiarabu wanakubaliana ya kuwa *Tawaffa* kama linavyotumika hapa haliwezi kuwa na tafsiri nyingine. Wanachuoni na Mufasirina mashuhuri kama (1) Ibni Abbas, (2) Imam Malik, (3) Imam Bukhari, (4) Imam Ibni Hazm, (5) Imam Ibni Kayyim, (6) Katada, (7) Wahab na wengineo, wanakubali jambo hili. (Tazama, 1. Bukhari, sura Tafsiri; 2. Bukhari, sura *Bad'ul Khalq;* 3. Bihar; 4. Al-Muhalla, Cairo, 1:23; 5. Ma'aad, uk. 19; 6. Manthur ii; 7. Kathir).

Fat'hul Bayaan kinasema, "Hao mufasirina ambao wamejaribu kutia maana nyingine katika neno *Tawaffa* linavyotumika kwa namna hiyo, wamefanya hivyo kwa sababu ya kusadiki kwao kuwa Yesu amepandishwa mbinguni hai; waila, neno hili halina maana nyingine isipokuwa maana ya kuchukua roho au kufisha." Tamko hili limetumiwa mahali pasipopungua 25 katika Qur'an na mahali pasipopungua 23 lina maana ya kuchukua roho wakati wa kufa. Mahali pawili tu limekuwa na maana ya kuchukua roho wakati wa kulala; lakini hapo limefuatana na neno "usingizi" au "usiku" (sura 6:61; 39:43).

Allama Alusi, mtungaji wa tafsiri iitwayo *Ruuhul-Ma'aani* amekubali ya kuwa *tawaffa* maana yake ni kifo.

فَاَمَّا الَّذِيْنَ كَفَرُوْا فَاُعَذِّبُهُمْ عَذَابًا شَدِيْدًا فِى الدُّنْيَا وَالْاٰخِرَةِ ۫ وَمَا لَهُمْ مِّنْ نّٰصِرِيْنَ ﴿٥٧﴾

57. Na ama wale waliokufuru, basi Nitawaadhibu adhabu kali katika dunia na Akhera, wala hawatapata wasaidizi.

وَاَمَّا الَّذِيْنَ اٰمَنُوْا وَعَمِلُوا الصّٰلِحٰتِ فَيُوَفِّيْهِمْ اُجُوْرَهُمْ ؕ وَاللّٰهُ لَا يُحِبُّ الظّٰلِمِيْنَ ﴿٥٨﴾

58. Na ama wale walioamini na kufanya vitendo vizuri, basi Yeye Atawalipa ujira wao sawasawa. Na Allah Hawapendi wadhalimu.

ذٰلِكَ نَتْلُوْهُ عَلَيْكَ مِنَ الْاٰيٰتِ وَالذِّكْرِ الْحَكِيْمِ ﴿٥٩﴾

59. Haya Tunayokusomea ni katika Aya na mawaidha yenye hekima.

Katika gazeti la Misri liitwalo *Arrisaalat war-Riwaayat* la tarehe 11 May, 1942, jalada 10, nambari 462, ukurasa 515, Sheikh Mahmud Shaltut ambaye ni mwanachuoni mkubwa wa Misri, na tena yu mwanachama wa Halmashauri ya kutoa Fat'wa katika Chuo Kikuu cha Azhar, amesema, "Neno *tawaffa* lililotumiwa katika Qur'an juu ya Nabii Isa lina maana ya kufa kwa kawaida."

Raafi'uka, "Nitakuinua." Neno *Rafa'* linapotumiwa kwa Allah kumpa mtu *Rafa'* halina maana nyingine isipokuwa "kutukuza." Mathlan Mtume *s.a.w.* amesema: *Innallaaha yarfa'u bihaadhal-Qur'ani aqwaaman wayadha'u aqwaaman,* yaani, Allah atawainua watu kwa Qur'an hii na wengine atawadhalilisha (Ibni Majah). Tena akasema: *Man tawaaadha'a lillahi rafa'ahullaahu ilassamaaisaabi'ati,* yaani, mtu anayenyenyekea kwa Allah, Mungu atamwinua mpaka mbingu ya saba, yaani atampa daraja ya juu kabisa ya kiroho ('Ummal, ii. 25). Allah amesema katika Qur'an, *Fii buyuutin adhinallaahu an turfa'a* yaani, "Katika nyumba ambazo Allah Ameruhusu zinyanyuliwe" (sura 24:37). Tena, *Wal'amalussaalihu yarfa'uhuu,* yaani, "Na kitendo kizuri huyapandisha" (sura 35:11). Katika Sala zetu kila siku tunasoma, *Allaahummarfa'nii,* yaani, "Ee, Mola nitukuze." Hivyo kupandisha huku ni kutukuza tu siyo kupeleka mbinguni kiwiliwili.

Kuwa Nabii Isa amekufa ni jambo la hakika kabisa lisilo na kinyume. Na kusema amepanda mbinguni ndiyo si kweli hata kidogo. Mtume *s.a.w.* amesema, "Musa na Isa wangekuwa hai wasingekuwa na njia ila kunifuata" (Kathir). Hata alisema umri wa Nabii Isa ulikuwa miaka 120 ('Ummal). Qur'an imevunja kabisa itikadi hii ya kupanda Isa mbinguni hai katika Aya zisizopungua 30.

Kama kusadiki Nabii Isa amepanda mbinguni kuna faida yo yote, basi labda wamepata Wakristo, ingawa kwa hakika hata kwao jambo hili ni sababu iliyowatia katika kufuru na hasara, kwani wamesaidiwa kuzidisha mkazo juu ya uungu wa Yesu wakisema, ni mwanadamu gani mwingine anayekaa hai mbinguni kwa miaka elfu mbili, asiyechakaa kwa uzee, asiyekula nafaka za ardhini, asiyelala na asiyekwenda choo, na asiyekufa kwa miaka yote hiyo? Wanapokuta hizi fikira zao zinatiwa nguvu na itikadi za Waislamu ambao kwa hakika waliziambukizwa na Ukristo, basi ndipo wanazidi imara. Hivyo ushirikina unazidi duniani, na kufuru kubwa ya kumfanya mtu kuwa Mungu inaendeshwa bila wasiwasi, na pembeni kumekaa baadhi ya Waislamu, wanaoupulizia moto huu uzidi kuwaka na wanauchochea. Waislamu kama asemavyo Seyyidna Ahmad, wamefanana na mtu anayekaa juu ya mti anakata shinani. Zaidi ya hayo, itikadi hii dhahiri iko kinyume na maneno ya Allah na Sunna ya Mtume Muhammad *s.a.w.*

60. Bila shaka mfano wa Isa kwa Allah ni kama mfano wa Adamu; Alimwumba kwa udongo kisha Akamwambia: kuwa, basi akawa.

اِنَّ مَثَلَ عِيْسٰى عِنْدَ اللّٰهِ كَمَثَلِ اٰدَمَ ؕ خَلَقَهٗ مِنْ تُرَابٍ ثُمَّ قَالَ لَهٗ كُنْ فَيَكُوْنُ ۝٦٠

Aya 60. *Hali ya Isa.* Kwa kusema hayo Allah anataka kuelekeza fikara za watu kwenye jambo kubwa mno. Mungu hafanani na mtu au kitu kingine katika viumbe Vyake. Kama Yesu alikuwa Mungu au mwanawe wa pekee, kama wadhanivyo Wakristo, mbona hali yake na tabia yake ilikuwa ni hali na tabia ya kibinadamu tu? Alizaliwa, alinyonya, alikula, alilala, alitembea, aliomba, aliadhibiwa na watu, na pia alikufa. Hayo yote ni mambo yanayohusiana na binadamu. Mungu ameepukana na kuzaliwa na kusikia maumivu na kufa.

YESU HANA SIFA ZA MUNGU

Sifa zipatikanazo katika dhati ya Allah, Yesu hakuwa nazo asilan:-

(1) Mungu ni Mweza wa yote, lakini Yesu hakuwa na uwezo huo. Safari moja mtu mmoja alileta watoto wake wawili kwa Yesu akataka Yesu akubali ya kuwa watakaa pamoja naye katika ufalme wake, mmoja kushoto na mwingine kulia. Yesu alijibu, kukalia kwangu kuume au kushoto si shauri langu kuwapa ninyi, ila wale waliowekewa na Baba yangu" (Matei 20:23). Tena alisema. "Mimi siwezi kufanya lo lote kwa amri yangu." (Yohana 5:30). Hayo yote yanaonyesha Yesu hakuwa na uwezo wala amri, bali alikuwa mtumishi wa Mungu kama wengine.

(2) Mungu ni Mjuzi wa yasiyoonekana. Yesu anakubali ya kwamba hana elimu ya ghaibu. Anasema: Siku yenyewe lakini, au saa yenyewe, hakuna mtu ajuaye wala malaika mbinguni, hata mwana ila baba peke yake" (Marko 13:32). Siku moja alikuwa katika mkutano wa watu na mwanamke mmoja alimgusa asitambue, akauliza, "Nani amenigusa?" (Luka 8:45).

(3) Mungu ni mwema. Lakini Yesu anakiri mwenyewe ya kwamba yeye si mwema. "Mtu mmoja wa maana akamwuliza, Mwalimu mwema, nifanye nini nipate uzima wa milele? Yesu akamwambia: Waniita mwema kwa nini? Hakuna mwema ila Mungu" (Luka 18:18,19).

(4) Allah ni mkubwa kuliko wote. Lakini Yesu anasema waziwazi ya kwamba "Baba ni mkubwa kuliko mimi" (Yoani 14:28). Ni dhahiri ya kuwa Yesu hakudai ukubwa kama Mungu, ingawa Mapadre wanapenda sana kumshirikisha sana katika mambo yote: uwezo, utukufu na mengineyo (Book of Common Prayer. Imani ya Athanasius Mt.).

KUZALIWA PASINA BABA SI DALILI YA UUNGU

Wakristo wanaleta dalili chache kutaka kuthibitisha uungu wa Yesu, kama kuzaliwa pasipo baba na kuonyesha miujiza na kufufuka katika wafu.

Kuzaliwa na mwanamke peke yake hakumfanyi mtu mwana wa Mungu. Adamu inasema Biblia, hakuzaliwa na baba wala mama. Na kulikuwa mtu mwingine, Melkizedeki, ambaye hakutokana na wazazi wo wote. Melkizedeki huyo. "hana baba, hana mama, hana wazazi, hana mwanzo wa siku zake, wala mwisho wa uhai wake, bali amefananishwa na Mwana wa Mungu" (Waebrania 7:3).

Hayo maneno ya Paulo yanafahamisha ya kuwa Yesu hakuwa peke yake katika kukosa baba, bali alipitwa hata na Melkizedeki aliyekuwa hana baba wala mama. Na wale wanaodhani kuwa Yesu ndiye Melkizedeki na wakumbuke ya kuwa Yesu alizaliwa na Mariamu, na zaidi ya hayo mtu hafananishwi na nafsi yake.

MIUJIZA PIA SI DALILI YA UUNGU

Hali ya miujiza ya Yesu pia ni kama hivyo. Biblia inashuhudia ya kwamba miujiza mingi ilionyeshwa na watu wa zamani ambao hawakubaliwi kuwa waungu: (1) Nabii Ezekiel alifufua jeshi kubwa mno la watu waliobaki mifupa mitupu (Ezekieli 37:1-10). (2) Nabii Elisha aliongeza kikombe kimoja tu cha mafuta nayo yakawa mengi, hata vikajazwa nayo vyombo vingi (2 Wafalme 4:1-7). (3) Nabii Joshua alipochelewa sana katika kupigana vita na maadui na usiku ulikaribia, aliliambia jua kusimama, na mwezi kutulia, na vyote viwili vikamtii (Joshua 10:12-13). (4) Wadudu warukao waliomsumbua Firauni na watu wake walikwisha kwa maombi ya Musa (Kutoka 8:31); na miujiza mingine pia ilifanyika (tazama 9:12, 23, 33; 10:13, 19, 22; 14:21, 27; 15:25 na 17:6). (5) Naaman aliyekuwa na ugonjwa wa ukoma alipona kwa kujiosha ndani ya mto wa Jordan (2 Wafalme 5:14). (6) Watu ambao hawakuwa Manabii kama Shadrakha, Meshakha na Abedinego walitupwa katika tanuri la moto kwa amri ya mfalme Bukhtanassar, na moto ule haukugusa hata nywele za vichwa vyao (Danieli 3:20-27).

(7) Siyo watu peke yao walioonyesha ishara kubwa kubwa, hata na vitu kama fimbo, nyoka wa shamba na shuka vilifanya vioja. Fimbo ya Nabii Harun inasemwa na Biblia kuwa ilimeza fimbo za wachawi wa Firauni (Kutoka 7:12). Na siku nyingine ile fimbo yake ilionekana kama imechipuza na kutoa lozi mbivu (Hesabu 17:8). Na Musa alifanya nyoka wa shaba, na imehadithiwa ya kwamba aliyeumwa na nyoka alipotazama tu yule nyoka wa shaba mara akapona (Hesabu 21:8, 9). Elisha alipopiga mto wa Yordani kwa shuka ya Elijah mara maji yake yaligawanyika , naye akavuka (2 Wafalme 2:14).

(8) Injili inasimulia ya kwamba katika mji wa Yerusalem palikuwa na birika la kuogea. "Watu wengi sana walikuwa wakilala pale, wagonjwa, vipofu, viguru, na waliopooza, wote wakingoja maji yachemke. Kwa sababu mara kwa mara Malaika wa Mungu hushuka kwenye birika, ndipo maji yake huanza kuchemka. Na mtu wa kwanza mwenye kushuka majini yakiisha kuchemka vile, hupona ugonjwa wote alionao" (Yoan 5:3-4).

(9) Injili inasadiki ya kwamba Wakristo wa uwongo pia wanaweza kufanya miujiza ya namna mbalimbali. Yesu alisema, "Siku ile wengi wataniambia: Bwana, Bwana we, hatukufanya unabii kwa jina lako? Hatukufukuza mashetani kwa jina lako? Hatukufanya miujiza mingi kwa jina lako? Lakini mimi nitawajibu kwamba sikuwajua ninyi hata siku moja. Ondokeni mbele yangu, mnatenda maovu" (Matei 7:22, 23). Kadhalika Injili inasema waziwazi ya kwamba inawezekana kufanya miujiza kwa nguvu ya Beelzebub, ambaye ni mkuu wa pepo wachafu (Matei 12:27). Kwa sababu hii Waislamu hawajali miujiza mingimingi inayosimuliwa na Wakristo kila mara. Ni vigumu sana kutambua ukweli wa mtu kwa kuponya mgonjwa tu. Siku hizi watu ambao hawana dini yo yote wanapona magonjwa ya namna nyingi kwa ustadi wao kwa elimu ya *Mesmerism* na *Hypnotism.*

Ama kusema ya kuwa hao Manabii wa kabla ya Yesu walifanya miujiza kwa nguvu ya Mungu, na Yesu alifanya kwa nguvu zake mwenyewe, si kweli. Maana hata Injili inakubali ya kuwa Yesu naye alifanyiwa miujiza yake na Mungu. Imeandikwa, "Watu wa Israeli, sikilizeni maneno haya: Mnajua wenyewe kwamba Yesu wa Nazareti alikuwa kati yenu kama mtu aliyeshuhudiwa na Mungu mwenyewe, kwa matendo ya ezi kuu, kwa *miujiza na kwa ishara, alizotenda Mungu kwenu kwa mkono wake"* (Matendo 2:22)

(10) Injili inaeleza jambo jingine lililo kubwa mno. Inasema, "Watakaosadiki watafuatwa na ishara hizi: kwa jina langu watawafukuza mashetani, watasema lugha nyingine, wataokota nyoka, na wakinywa sumu haitawadhuru, watawawekea wagonjwa mikono, nao watapona" (Marko 16:17, 18). Kama kusema lugha nyingine inawezekana baada ya kujifunza, basi siyo ishara. Na kama Mkiristo aweza kusema tu kwa jina la Yesu, basi tutapenda kuzungumza na Mkristo huyo lugha kama, Kiarabu, Kihindi na nyingine. Wakristo wanaosadiki imani ya Kikristo wangefanya vizuri kuponya watu walio wagonjwa kwa kuwawekea mikono tu na bila kuchukua kwao pesa. Ingekuwa msaada mkubwa kwa maskini na wenye maradhi.

Haitakiwi imani kubwa kwa Wakristo kufanya miujiza. Yesu aliwaambia, "Nasema kweli,

61. Hiyo ni haki iliyotoka kwa Mola wako, basi usiwe miongoni mwa wenye shaka.

اَلْحَقُّ مِنْ رَّبِّكَ فَلَا تَكُنْ مِّنَ الْمُمْتَرِيْنَ ﴿٦١﴾

62. Lakini atakayekuhoji katika hayo baada ya kukufikia elimu, basi sema: Njooni tuwaite watoto wetu, na watoto wenu, na wake zetu na wake zenu, na watu wetu na watu wenu; kisha tuombe kwa unyenyekevu na kuiweka laana ya Allah juu ya waongo.

فَمَنْ حَآجَّكَ فِيْهِ مِنْۢ بَعْدِ مَا جَآءَكَ مِنَ الْعِلْمِ فَقُلْ تَعَالَوْا نَدْعُ اَبْنَآءَنَا وَاَبْنَآءَكُمْ وَنِسَآءَنَا وَنِسَآءَكُمْ وَاَنْفُسَنَا وَاَنْفُسَكُمْ ۟ ثُمَّ نَبْتَهِلْ فَنَجْعَلْ لَّعْنَتَ اللّٰهِ عَلَى الْكٰذِبِيْنَ ﴿٦٢﴾

---

mngalikuwa na imani ndogo kama chembe ya hardali, mngesema kwa mlima huu: Ondoka hapa nenda kule, utaondoka. Hakutakuwa na jambo lo lote lisilowezekana kwenu" (Matei 17:19, 20). Je, Hakuna katika Wakristo wote wa dunia nzima mmoja aliye na imani kama punje ya hardali akatuonyesha vioja vinavyotajwa na aya hii ya Injili?

Si hayo tu. Yesu alisema, "Namwambieni hakika kabisa kwamba mwenye kuniamini atafanya matendo yale nitendayo mimi; hata atatenda makubwa zaidi" (Yoani 14:12). Mambo yamekuwa rahisi sana . Waislamu hawana haja ya kutishwa na miujiza ya Yesu, wawaulize tu wafuasi wake kufanya yale yale wanayokiri wenyewe katika Injili zao kuwa wanaweza kuyafanya. Kama wao wenyewe watashindwa kufanya yale ambayo Vitabu vyao vinasema watayaweza, basi ya nini wao kusema mambo yasiyosadikika?

Kwa neno zima, maneno ya juu yamekwisha hakikisha bila shaka hata kidogo ya kuwa Yesu hawezi hata kidogo kuitwa Mungu kwa sababu ya vioja na miujiza anayosemwa kuwa alifanya. Na kwa usemi wa Injili, mtu hata si Nabii wa kweli kwa kufanya miujiza tu. Lakini kama Wakristo watashikilia tu kuwa ni Mungu kwa sababu ya miujiza, basi itawalazimu wakubali uungu wa kila aliyefanya miujiza: toka Manabii wa zamani, watu tu, vitu kama fimbo na maji n.k.w. Na pia italazimu wakubali kuwa miungu, wale manabii wa uwongo wanaofanya miujiza (Matt. 24:24). Hivyo shauri limekwisha katika ya kuwa Yesu hawezi kuwa Mungu kwa sababu ya miujiza anayosifiwa kuwa alifanya.

Tumeieleza kidogo Aya hii ya Qur'an. Tungeweza kueleza zaidi, lakini hayo yatosha kumfikirisha Mkristo. Tukizidi kupeleleza habari za Yesu itazidi kubainika ya kwamba hali yake ni hali ya wanadamu tu. Hawezi kuwa Mungu au mwanawe wa pekee. (Kwa maelezo ya kufufuka kwake tazama sura 4:158).

Aya 62. Habari zinazohusu itikadi za Wakristo zilizoanza katika sura hii zinakoma katika Aya hii. Aya hii inahusu ujumbe wa Wakristo waliotoka Najran uliokuwa na watu 60 chini ya mkubwa wao Abdul Masih, anayeitwa Al'Aakib. Walikuta na Mtume *s.a.w.* katika msikiti wake na majadiliano juu ya uungu wa Yesu yakaendelea kwa muda mrefu. Jambo hili lilipozungumzwa kwa kutosheleza kabisa na wale Wakristo wakaendelea kushikilia itikadi yao ya uwongo, Mtume s.a.w. akaamrishwa na Allah katika Aya hii kuwataka washindane katika maombi kuwa jambo la mwisho. Mashindano haya ya kuomba dua huitwa *mubaahala,* yaani kuiita laana ya Mungu impige anayeshika itikadi za uwongo. Lakini kwa kuwa Wakristo walikuwa hawana hakika na itikadi zao walikataa kupokea mashindano haya, na hivyo ikawa kama wamekiri uwongo wa itikadi zao (Zurkani, Khamis na Bayan, katika maelezo ya sura 3:3).

63. Kwa yakini hayo ndiyo maelezo ya kweli, na hakuna aabudiwaye ila Allah; na hakika Allah ndiye Mwenye ushindi kamili, Mwenye hekima.

إِنَّ هَٰذَا لَهُوَ الْقَصَصُ الْحَقُّ ۚ وَمَا مِنْ إِلَٰهٍ إِلَّا اللَّهُ ۚ وَإِنَّ اللَّهَ لَهُوَ الْعَزِيزُ الْحَكِيمُ ﴿٦٣﴾

Katika tukio hili Mtume *s.a.w.* alimleta Ali, Fatima, Hassan na Hussein (Khamis na Zurkani) na pia Abubakar, Umar, Uthman na wengine ('Asakir) uwanjani, na akasema: "Kama Wakristo wangekubali mashindano ya *mubaahala* na kukubali kumwomba Mungu kushusha adhabu yake juu ya kundi linalozua uwongo, Allah bila shaka angewaangamiza waongo kabla ya mwaka haujamalizika" (Bukhari, Muslim na Tirmidhi).

SHARTI ZA MUBAHALA

Mubahala ni jambo zito na kubwa kabisa na halishikwi ovyo, bali katika matokeo ya namna ya pekee kabisa. Sharti zake zinazotokana na Aya hii na maneno ya Mtume *s.a.w.* ni tano: (1) Jambo linalobishaniwa liwe jambo kubwa kabisa katika dini na linaloelezwa kwa ushahidi ulio wazi wa Kitabu cha dini. (2) Jambo hilo kwanza liwe limekwisha bishaniwa kwa kiasi cha kutosha na hizo pande mbili zinazojadiliana. (3) Mubahala ufanyike ikiwa baada ya majadiliano hayo kila upande unaendelea kushikilia maoni yake na kuuona upande wa pili kuwa ndiyo wenye kosa. (4) Kwa ajili ya mashindano hayo, pande hizo mbili wakutane mahali pamojapo, pamoja na ahli zao, pamoja na idadi nyingine ya watu wanaoshikilia maoni ya namna hiyo, kisha kuomba kwa unyenyekevu laana ya Mungu iwashukie walio waongo. (5) Muda wa kungojea matokeo ya adhabu juu ya uwongo uwe mwaka mmoja.

Dini ya Kiislamu haitaki kuwacha shaka yo yote katika moyo wa mtu juu ya ukweli wa dini. Hivyo, imetumia njia zote - toka za hoja na dalili za akili, mpaka ahadi za Vitabu - kuhakikisha ukweli wa Uislamu. Na sasa imeleta njia nyingine moja ili kuamua mabishano ya mataifa ya dini, watu wote wapate kuwa na hakika ukweli uko wapi.

KUOMBEA LAANA HIVYO SI AIBU.

Padre Dale anasema, "Mfuasi wa dini ya kweli hamlaani mwenzake" (uk. 564 wa Tafsiri yake ya Qur'an). Lakini hapa si kulaani ovyo bali ni mashindano ya kupeleka kesi kwa Allah akate hukumu, baada ya kuwa watu wenyewe wamekwisha shindana na hawana mwamuzi.

Zaidi ya hayo, ikiwa ni kweli "mfuasi wa dini ya kweli hamlaani mwenzake," ilikuwaje mfuasi wa dini ya kweli kama Daudi, babu wa Yesu, kuwalaani wenzake kwa maneno haya: "Wamiminie ghadhabu zako juu yao, na wakumbwe na hasira zako motomoto" (Zaburi 69-24). Je, maneno haya ni kulaani au kuombea rehema? Na kama usome Zaburi 109:6-15 ndiyo utazidi kuchoka. Mtu mmoja analaaniwa na Daudi kwa maneno haya: "Maombi yake yawe dhambi" (7). "Siku zake ziwe chache" (8). "Wanawe wawe mayatima na mkewe awe mjane" (9). "Kizazi chake kikatwe" (13). "Upotofu wa babaze ukumbukwe kwa Mungu" (14). "Na dhambi ya mama yake isifutike" (15) na mengineyo kadha wa kadha. Kulaani mtu namna hii Padre Dale atasema ni kwa sababu Daudi alikuwa mfuasi wa dini ya uwongo?

Kadhalika Yesu anasemwa aliulaani mtini kwa sababu ya njaa alipokuta hauna matunda, akauapiza usizae (Matt. 21:19). Yesu huyo huyo akamlaani Petro, mwanafunzi wake, kwa kumwambia, "Fuata nyuma shetani, wanichukiza" (Matei 16:23). Na Petro huyo ambaye anasemwa alikabidhiwa na Yesu funguo za mbinguni (Matt. 16:19). alilaani na kuapiza kuwa hamjui Yesu (Marko 14:71).

Katika mambo madogo madogo wanajua sana kulaani, lakini kwa kuhakikisha ukweli wa dini wanajitia hamnazo kwa kusema, "Mfuasi wa dini ya kweli hamlaani mwenzake"! Kujipurukusha kwa namna hii hakufai kitu mbele ya haki.

فَاِنْ تَوَلَّوْا فَاِنَّ اللّٰهَ عَلِيْمٌۢ بِالْمُفْسِدِيْنَ ﴿٦٣﴾ ع ١٤

64. Na kama wakigeuka, basi kwa hakika Allah ni Mwenye kuwajua waharibifu.

FUNGU 7

قُلْ يٰٓاَهْلَ الْكِتٰبِ تَعَالَوْا اِلٰى كَلِمَةٍ سَوَآءٍۢ بَيْنَنَا وَبَيْنَكُمْ اَلَّا نَعْبُدَ اِلَّا اللّٰهَ وَلَا نُشْرِكَ بِهٖ شَيْـًٔا وَّلَا يَتَّخِذَ بَعْضُنَا بَعْضًا اَرْبَابًا مِّنْ دُوْنِ اللّٰهِ ؕ فَاِنْ تَوَلَّوْا فَقُوْلُوا اشْهَدُوْا بِاَنَّا مُسْلِمُوْنَ ﴿٦٤﴾

65. Sema: Enyi watu wa Kitabu, njooni kwenye neno lililo sawa baina yetu na baina yenu, ya kwamba hatutamwabudu ye yote ila Allah, wala hatutamshirikisha na cho chote, wala baadhi yetu hatutawafanya wengine kuwa waungu badala ya Allah; lakini wakigeuka, basi semeni: Shuhudieni ya kwamba sisi ni Waislamu.

يٰٓاَهْلَ الْكِتٰبِ لِمَ تُحَآجُّوْنَ فِيْٓ اِبْرٰهِيْمَ وَمَآ اُنْزِلَتِ التَّوْرٰىةُ وَالْاِنْجِيْلُ اِلَّا مِنْۢ بَعْدِهٖ ؕ اَفَلَا تَعْقِلُوْنَ ﴿٦٥﴾

66. Enyi watu wa Kitabu, mbona mnabishana juu ya Ibrahimu na hali Taurati na Injili havikuteremshwa ila baada yake; basi je, hamfahamu?

هٰٓاَنْتُمْ هٰٓؤُلَآءِ حَاجَجْتُمْ فِيْمَا لَكُمْ بِهٖ عِلْمٌ فَلِمَ تُحَآجُّوْنَ فِيْمَا لَيْسَ لَكُمْ بِهٖ عِلْمٌ ؕ وَاللّٰهُ يَعْلَمُ وَاَنْتُمْ لَا تَعْلَمُوْنَ ﴿٦٦﴾

67. Angalieni! ninyi ndio mliobishana katika yale mliyoyajua; tena mbona mnabishana katika yale msiyoyajua? Na Allah Anajua lakini ninyi hamjui.

مَا كَانَ اِبْرٰهِيْمُ يَهُوْدِيًّا وَّلَا نَصْرَانِيًّا وَّلٰكِنْ كَانَ حَنِيْفًا مُّسْلِمًا ؕ وَمَا كَانَ مِنَ الْمُشْرِكِيْنَ ﴿٦٧﴾

68. Ibrahimu hakuwa Myahudi wala Mkristo, lakini alikuwa mwongofu, mtii, wala hakuwa miongoni mwa washirikina.

اِنَّ اَوْلَى النَّاسِ بِاِبْرٰهِيْمَ لَلَّذِيْنَ اتَّبَعُوْهُ وَهٰذَا النَّبِيُّ وَالَّذِيْنَ اٰمَنُوْا ؕ وَاللّٰهُ وَلِيُّ الْمُؤْمِنِيْنَ ﴿٦٨﴾

69. Hakika watu wanaomkurubia zaidi Ibrahimu ni wale waliomfuata yeye na Mtume huyu na walioamini; na Allah ndiye Rafiki wa waaminio.

وَدَّتْ طَّآئِفَةٌ مِّنْ اَهْلِ الْكِتٰبِ لَوْ يُضِلُّوْنَكُمْ ؕ وَمَا يُضِلُّوْنَ اِلَّآ اَنْفُسَهُمْ وَمَا يَشْعُرُوْنَ ﴿٦٩﴾

70. Kundi moja miongoni mwa watu wa Kitabu wanapenda laiti wangewapotezeni, lakini hawapotezi ila nafsi zao hali hawatambui.

Aya 70. *Yudhilluunakum,* "Wangewapotezeni," pia linaweza kufasiriwa. "Wangewaangamizeni." Neno la dhalaalah linakuwa na maana ya "kuangamiza" pia (Akrab). Maneno ya baadaye, *Hawapotezi ila nafsi zao,* yatakuwa na maana ya kuwa badala ya kuwaangamiza Waislamu, wao wanajiangamiza wenyewe; maana kuinuka kwa adui yako ndiko kuanguka kwako.

71. Enyi watu wa Kitabu, mbona mnazikataa Aya za Allah hali mnashuhudia?

يٰٓاَهۡلَ الۡكِتٰبِ لِمَ تَكۡفُرُوۡنَ بِاٰيٰتِ اللّٰهِ وَاَنۡتُمۡ تَشۡهَدُوۡنَ ﴿۷۱﴾

72. Enyi watu wa Kitabu, mbona mnachanganya haki na batili, na mnaficha haki hali mnajua?

يٰٓاَهۡلَ الۡكِتٰبِ لِمَ تَلۡبِسُوۡنَ الۡحَقَّ بِالۡبَاطِلِ وَتَكۡتُمُوۡنَ الۡحَقَّ وَاَنۡتُمۡ تَعۡلَمُوۡنَ ﴿۷۲﴾ ع ۸

FUNGU 8

73. Na kundi moja katika watu wa Kitabu likasema: Aminini yaliyoteremshwa juu ya wale walioamini, mwanzo wa mchana, na mkatae mwisho wake, huenda wakarejea;

وَقَالَتۡ طَّآئِفَةٌ مِّنۡ اَهۡلِ الۡكِتٰبِ اٰمِنُوۡا بِالَّذِىۡۤ اُنۡزِلَ عَلَى الَّذِيۡنَ اٰمَنُوۡا وَجۡهَ النَّهَارِ وَاكۡفُرُوۡۤا اٰخِرَهٗ لَعَلَّهُمۡ يَرۡجِعُوۡنَ ﴿۷۳﴾

74. Wala msimwamini ye yote isipokuwa yule anayefuata dini yenu. Sema: Bila shaka mwongozo hasa ni mwongozo wa Allah (sio lazima kwamba) yeyote apewe kile kile mlichopewa. (Vinginevyo watakuwa na haki ya) kutoa hoja dhidi yenu mbele ya Mola wenu. Sema: Hakika fadhili zi mkononi mwa Allah, Humpa Amtakaye; na Allah ni Mwenye kutoa sana wasaa na Mwenye elimu ya kudumu.

وَلَا تُؤۡمِنُوۡۤا اِلَّا لِمَنۡ تَبِعَ دِيۡنَكُمۡ ؕ قُلۡ اِنَّ الۡهُدٰى هُدَى اللّٰهِ ۙ اَنۡ يُّؤۡتٰٓى اَحَدٌ مِّثۡلَ مَاۤ اُوۡتِيۡتُمۡ اَوۡ يُحَآجُّوۡكُمۡ عِنۡدَ رَبِّكُمۡ ؕ قُلۡ اِنَّ الۡفَضۡلَ بِيَدِ اللّٰهِ ۚ يُؤۡتِيۡهِ مَنۡ يَّشَآءُ ؕ وَاللّٰهُ وَاسِعٌ عَلِيۡمٌ ﴿۷۴﴾

75. Humchagua kwa rehema Zake Amtakaye; na Allah ndiye Mwenye fadhili kubwa.

يَّخۡتَصُّ بِرَحۡمَتِهٖ مَنۡ يَّشَآءُ ؕ وَاللّٰهُ ذُو الۡفَضۡلِ الۡعَظِيۡمِ ﴿۷۵﴾

Aya 74. Aya hii yaonyesha kwamba sio Mayahudi waliokuwa na shauri la kuhoji dhidi ya Mtukufu Mtume s.a.w. kwa sababu eti mafundisho aliyopewa hayakuwa sawa moja kwa moja na yao. Bali kinyume na hivyo ingelikuwa haki ya umma wa Kiislamu kutoa hoja dhidi yao hao Mayahudi kama hawa Waislamu wangalinyimwa moja kwa moja mafundisho ya Mungu, jambo linaloonyesha uadilifu wa Allah kwa watu wa Kitabu. Kutofautiana kwa mafundisho ambako Mayahudi walikufanya kuwa ndiyo sababu ya kukataa kwao ni jambo lisilohusika hapa.

Aya 75. *Fadhili.* Neno fadhili hapa lina maana ya fadhili ya Unabii na ufunuo. Watu wa Kitabu wanaambiwa kuwa Allah Anapenda kuwapa watu wengine unabii na ufunuo; basi wao hawana sababu ya kunung'unika na kulalama.

76. Na katika watu wa Kitabu yuko ambaye ukimpa amana ya rundo la mali atakurudishia, na katika wao yuko ambaye ukiweka kwake amana ya dinari moja, hakurudishii isipokuwa uendelee kumsimamia. Haya ni kwa sababu walisema: Si lawama juu yetu kwa (mali ya) hawa wajinga; na wanasema uwongo juu ya Allah na hali wanajua.

وَمِنْ اَهْلِ الْكِتٰبِ مَنْ اِنْ تَاْمَنْهُ
بِقِنْطَارٍ يُّؤَدِّهٖۤ اِلَيْكَ ۚ وَمِنْهُمْ مَّنْ اِنْ
تَاْمَنْهُ بِدِيْنَارٍ لَّا يُؤَدِّهٖۤ اِلَيْكَ اِلَّا مَا دُمْتَ
عَلَيْهِ قَآئِمًا ؕ ذٰلِكَ بِاَنَّهُمْ قَالُوْا لَيْسَ
عَلَيْنَا فِى الْاُمِّيّٖنَ سَبِيْلٌ ۚ وَيَقُوْلُوْنَ عَلَى
اللّٰهِ الْكَذِبَ وَهُمْ يَعْلَمُوْنَ ﴿۷۵﴾

77. Naam, anayetekeleza ahadi yake na kujilinda na dhambi, basi hakika Allah Huwapenda wajilindao (na madhambi).

بَلٰى مَنْ اَوْفٰى بِعَهْدِهٖ وَاتَّقٰى فَاِنَّ اللّٰهَ
يُحِبُّ الْمُتَّقِيْنَ ﴿۷۶﴾

78. Hakika wale wanaouza ahadi ya Allah na viapo vyao kwa thamani ndogo, hao ndio hawatakuwa na sehemu katika Akhera, wala Allah Hatasema nao wala Hatawatazama siku ya Kiyama, wala Hatawatakasa, nao watapata adhabu iumizayo.

اِنَّ الَّذِيْنَ يَشْتَرُوْنَ بِعَهْدِ اللّٰهِ وَاَيْمَانِهِمْ
ثَمَنًا قَلِيْلًا اُولٰٓئِكَ لَا خَلَاقَ لَهُمْ فِى
الْاٰخِرَةِ وَلَا يُكَلِّمُهُمُ اللّٰهُ وَلَا يَنْظُرُ
اِلَيْهِمْ يَوْمَ الْقِيٰمَةِ وَلَا يُزَكِّيْهِمْ ۪ وَلَهُمْ
عَذَابٌ اَلِيْمٌ ﴿۷۷﴾

79. Na kwa yakini liko kundi moja miongoni mwao wanaopinda ndimi zao kwa (kusoma) Kitabu ili mpate kuyafikiri (maneno yao) kwamba ni ya Kitabu, na kumbe si ya Kitabu; na wanasema, haya yametoka kwa Allah, na hali hayakutoka kwa Allah; na wanasema uwongo juu ya Allah na hali wanajua.

وَاِنَّ مِنْهُمْ لَفَرِيْقًا يَّلْوٗنَ اَلْسِنَتَهُمْ
بِالْكِتٰبِ لِتَحْسَبُوْهُ مِنَ الْكِتٰبِ وَمَا هُوَ
مِنَ الْكِتٰبِ ۚ وَيَقُوْلُوْنَ هُوَ مِنْ عِنْدِ اللّٰهِ
وَمَا هُوَ مِنْ عِنْدِ اللّٰهِ ۚ وَيَقُوْلُوْنَ عَلَى
اللّٰهِ الْكَذِبَ وَهُمْ يَعْلَمُوْنَ ﴿۷۸﴾

Aya 76. *Si lawama juu yetu.* Mayahudi katika siku za Mtume s.a.w. walikuwa na fikira iliyoenea kati yao ya kuwa si dhambi kuwanyang'anya Waarabu mali zao, maana Waarabu walifuata dini ya uwongo. Basi hapa Allah Anawalaumu. Katika nchi hii pia ni masikitiko kuona baadhi ya Waislamu wanadhani kuwa si haramu kudhulumu mali za makafiri. Tendo hili ni dhambi kubwa. Dhuluma ni dhuluma tu kwa ye yote anayedhulumiwa hata awe nani.

Aya 77. Katika Aya hii waaminio wanapewa mawaidha wasifuate mfano mbaya wa Mayahudi bali wawatendee watu kwa uadilifu, watimize ahadi zao na kila namna ya mapatano.

مَا كَانَ لِبَشَرٍ اَنْ يُّؤْتِيَهُ اللّٰهُ الْكِتٰبَ
وَالْحُكْمَ وَالنُّبُوَّةَ ثُمَّ يَقُوْلَ لِلنَّاسِ
كُوْنُوْا عِبَادًا لِّيْ مِنْ دُوْنِ اللّٰهِ وَلٰكِنْ
كُوْنُوْا رَبّٰنِيّٖنَ بِمَا كُنْتُمْ تُعَلِّمُوْنَ
الْكِتٰبَ وَبِمَا كُنْتُمْ تَدْرُسُوْنَ ﴿٧٩﴾

80. Haiwezekani kwa mtu kwamba Allah Ampe Kitabu na hekima na Unabii kisha aseme kwa watu: Kuweni watumishi wangu badala ya kuwa watumishi wa Allah; bali atasema: Kuweni wenye kujitoa wakfu kwa Mola kwa sababu mnafundisha Kitabu, na kwa sababu mnakisoma.

وَلَا يَاْمُرَكُمْ اَنْ تَتَّخِذُوا الْمَلٰٓئِكَةَ
وَالنَّبِيّٖنَ اَرْبَابًا ؕ اَيَاْمُرُكُمْ بِالْكُفْرِ بَعْدَ
اِذْ اَنْتُمْ مُّسْلِمُوْنَ ﴿٨٠﴾ ع ١٢

81. Wala yeye hatawaamuruni kuwafanya Malaika na Manabii kuwa waungu; je, atawaamuruni ninyi kufuru baada ya ninyi kuwa Waislamu.

FUNGU 9

وَاِذْ اَخَذَ اللّٰهُ مِيْثَاقَ النَّبِيّٖنَ لَمَآ اٰتَيْتُكُمْ
مِّنْ كِتٰبٍ وَّحِكْمَةٍ ثُمَّ جَآءَكُمْ رَسُوْلٌ
مُّصَدِّقٌ لِّمَا مَعَكُمْ لَتُؤْمِنُنَّ بِهٖ
وَلَتَنْصُرُنَّهٗ ؕ قَالَ ءَاَقْرَرْتُمْ
وَاَخَذْتُمْ عَلٰى ذٰلِكُمْ اِصْرِيْ ؕ قَالُوْٓا
اَقْرَرْنَا ؕ قَالَ فَاشْهَدُوْا وَاَنَا مَعَكُمْ
مِّنَ الشّٰهِدِيْنَ ﴿٨١﴾

82. Na (kumbukeni) Aliposhika Allah ahadi kwa Manabii: Nikiisha wapeni Kitabu na hekima, kisha awafikieni Mtume msadikishaji wa yale yaliyo pamoja nanyi, ni juu yenu kumwamini na kumsaidia. Akasema, Je, mmekubali na kushika agizo Langu juu ya hayo? Wakanena: Tumekubali. Akasema: Basi shuhudieni, na Mimi ni pamoja nanyi katika mashahidi.

فَمَنْ تَوَلّٰى بَعْدَ ذٰلِكَ فَاُولٰٓئِكَ هُمُ
الْفٰسِقُوْنَ ﴿٨٢﴾

83. Na atakayepinduka baada ya haya, basi hao ndiyo wavunjao amri.

Aya 80. *Rabbaaniyyin,* "Wenye kumwabudu Allah." Neno hili pia maana yake ni: mtu anayejitoa kufanya kazi ya dini tu au kufanya matendo ya ibada: mtu mwenye elimu ya Allah na ya mambo ya dini; mtu mwema na mtawa ; mwalimu wa watu anayeanza kuwafunza watu mambo madogo madogo kabla hawajaingia katika mambo makubwa; mtu mwenye cheo kikubwa katika elimu; kiongozi, mtumishi (Lane, Sibawaih na Mubarrad).

Aya 82. Aya hii inaeleza kanuni moja, kuwa kufika kwa kila Mtume huwa kumebashiriwa na Mtume aliyemtangulia. Kama Mtume yule kufika kwake kunatimiza mabashirio yaliyomo katika Vitabu vya taifa mojapo, kama alivyokuwa Yesu na Manabii wengine wa Kiisraeli, basi taifa lile tu ndilo linatakiwa kumkubali. Lakini kama Mtume huyo amebashiriwa katika Vitabu vya mataifa yote, kama alivyobashiriwa Mtume Muhammad *s.a.w.* basi mataifa hayo yote yatalazimika kumkubali na kumsaidia.

84. Je, wanataka dini isiyokuwa ya Allah, na hali kila kilichomo mbinguni na ardhini kinamtii Yeye, kikipenda kisipende? Na Kwake watarejeshwa.

اَفَغَيْرَ دِيْنِ اللّٰهِ يَبْغُوْنَ وَلَهٗۤ اَسْلَمَ مَنْ فِي السَّمٰوٰتِ وَالْاَرْضِ طَوْعًا وَّكَرْهًا وَّاِلَيْهِ يُرْجَعُوْنَ ﴿٨٣﴾

85. Sema: Tumemwamini Allah na yale tuliyoteremshiwa, na yaliyoteremshwa juu ya Ibrahimu na Ismaili na Isihaka na Yakubu na watoto (wake), na waliyopewa Musa na Isa na Manabii kutoka kwa Mola wao. Hatubagui baina yao hata mmoja, na sisi tunajitupa Kwake.

قُلْ اٰمَنَّا بِاللّٰهِ وَمَاۤ اُنْزِلَ عَلَيْنَا وَمَاۤ اُنْزِلَ عَلٰۤى اِبْرٰهِيْمَ وَاِسْمٰعِيْلَ وَاِسْحٰقَ وَيَعْقُوْبَ وَالْاَسْبَاطِ وَمَاۤ اُوْتِيَ مُوْسٰى وَعِيْسٰى وَالنَّبِيُّوْنَ مِنْ رَّبِّهِمْ ۖ لَا نُفَرِّقُ بَيْنَ اَحَدٍ مِّنْهُمْ ۚ وَنَحْنُ لَهٗ مُسْلِمُوْنَ ﴿٨٤﴾

86. Na anayetaka dini minghairi ya Islam , basi haitakubaliwa kwake, naye katika Akhera atakuwa miongoni mwa wenye hasara.

وَمَنْ يَّبْتَغِ غَيْرَ الْاِسْلَامِ دِيْنًا فَلَنْ يُّقْبَلَ مِنْهُ ۚ وَهُوَ فِي الْاٰخِرَةِ مِنَ الْخٰسِرِيْنَ ﴿٨٥﴾

87. Allah atawaongozaje watu waliokufuru baada ya kuamini kwao, na wakashuhudia ya kwamba Mtume ni haki, na kuwafikia dalili zilizo wazi? Na Allah Hawaongozi watu wadhalimu.

كَيْفَ يَهْدِي اللّٰهُ قَوْمًا كَفَرُوْا بَعْدَ اِيْمَانِهِمْ وَشَهِدُوْۤا اَنَّ الرَّسُوْلَ حَقٌّ وَّجَآءَهُمُ الْبَيِّنٰتُ ؕ وَاللّٰهُ لَا يَهْدِي الْقَوْمَ الظّٰلِمِيْنَ ﴿٨٦﴾

88. Hao ndio watu ambao malipo yao ni kuwa iko, juu yao laana ya Allah, na ya Malaika na ya watu wote.

اُولٰٓئِكَ جَزَآؤُهُمْ اَنَّ عَلَيْهِمْ لَعْنَةَ اللّٰهِ وَالْمَلٰٓئِكَةِ وَالنَّاسِ اَجْمَعِيْنَ ﴿٨٧﴾

89. Humo watakaa kwa muda mrefu. Hawatapunguziwa adhabu wala hawatapewa nafasi;

خٰلِدِيْنَ فِيْهَا ۚ لَا يُخَفَّفُ عَنْهُمُ الْعَذَابُ وَلَا هُمْ يُنْظَرُوْنَ ﴿٨٨﴾

90. Isipokuwa waliotubu baada ya hayo na wakasahihisha, basi hakika Allah ni Msamehevu Mrehemevu.

اِلَّا الَّذِيْنَ تَابُوْا مِنْۢ بَعْدِ ذٰلِكَ وَاَصْلَحُوْا ۗ فَاِنَّ اللّٰهَ غَفُوْرٌ رَّحِيْمٌ ﴿٨٩﴾

91. Hakika wale waliokufuru baada ya kuamini kwao, kisha wakazidi katika

اِنَّ الَّذِيْنَ كَفَرُوْا بَعْدَ اِيْمَانِهِمْ ثُمَّ ازْدَادُوْا كُفْرًا لَّنْ تُقْبَلَ تَوْبَتُهُمْ ۚ

Aya 90. *Waliotubu baada ya hayo na wakasahihisha.* Toba hasa ni ile ambayo mtu anatubu na anaacha kabisa maovu, kisha anatenda wema na anawaambia wengine kutenda wema.

Aya 91. *Toba yao haitakubaliwa*, yaani toba ya watu wale wanaosema kuwa wametubu lakini si kwa nia safi, na badala ya kujibadilisha maisha yao vizuri, wao wanaendelea kuzidi katika uovu.

وَاُولٰٓئِكَ هُمُ الضَّآلُّوْنَ ﴿٩١﴾

kufuru, toba yao haitakubaliwa kamwe, na hao ndiyo waliopotea.

اِنَّ الَّذِيْنَ كَفَرُوْا وَمَاتُوْا وَهُمْ كُفَّارٌ فَلَنْ يُّقْبَلَ مِنْ اَحَدِهِمْ مِّلْءُ الْاَرْضِ ذَهَبًا وَّلَوِ افْتَدٰى بِهٖ ؕ اُولٰٓئِكَ لَهُمْ عَذَابٌ اَلِيْمٌ وَّمَا لَهُمْ مِّنْ نّٰصِرِيْنَ ﴿٩٢﴾ ع ١٧

92. Hakika wale waliokufuru, na wakafa hali makafiri, basi haitakubaliwa kwa mmoja wao ijapokuwa atoe fidia ya dhahabu kwa kuijaza ardhi yote; hao ndiyo watakaopata adhabu iumizayo, wala hawatakuwa na wasaidizi.

JUZU 4

FUNGU 10

لَنْ تَنَالُوا الْبِرَّ حَتّٰى تُنْفِقُوْا مِمَّا تُحِبُّوْنَ ۬ ؕ وَمَا تُنْفِقُوْا مِنْ شَيْءٍ فَاِنَّ اللّٰهَ بِهٖ عَلِيْمٌ ﴿٩٣﴾

93. Hamtaweza kuufikia wema hasa mpaka mtoe katika vile mnavyovipenda; na cho chote mnachokitoa, basi hakika Allah Anakijua.

كُلُّ الطَّعَامِ كَانَ حِلًّا لِّبَنِيْٓ اِسْرَآءِيْلَ اِلَّا مَا حَرَّمَ اِسْرَآءِيْلُ عَلٰى نَفْسِهٖ مِنْ قَبْلِ اَنْ تُنَزَّلَ التَّوْرٰىةُ ؕ قُلْ فَاْتُوْا بِالتَّوْرٰىةِ فَاتْلُوْهَآ اِنْ كُنْتُمْ صٰدِقِيْنَ ﴿٩٤﴾

94. Kila chakula kilikuwa halali kwa wana wa Israeli, isipokuwa kile alichojiharamishia Israeli mwenyewe kabla haijateremshwa Taurati. Sema: Leteni Taurati na mwisome kama ninyi ni wakweli.

فَمَنِ افْتَرٰى عَلَى اللّٰهِ الْكَذِبَ مِنْۢ بَعْدِ ذٰلِكَ فَاُولٰٓئِكَ هُمُ الظّٰلِمُوْنَ ﴿٩٥﴾

95. Na ye yote amtungiaye uwongo Allah baada ya haya, basi hao ndiyo wadhalimu.

قُلْ صَدَقَ اللّٰهُ ۟ فَاتَّبِعُوْا مِلَّةَ اِبْرٰهِيْمَ حَنِيْفًا ؕ وَمَا كَانَ مِنَ الْمُشْرِكِيْنَ ﴿٩٦﴾

96. Sema: Allah Amesema kweli, basi fuateni mila ya Ibrahimu aliyehalisika, wala hakuwa miongoni mwa washirikina.

Aya 92. Kama moyoni hamna imani, kutoa sadaka tu au kufanya matendo yanayoonekana kuwa mema tu hakuwezi kumpatia mtu radhi ya Mungu hata kama atumie malundo ya dhahabu.

Aya 93. *Hamtaweza kuufikia wema.* Hapa neno maana hizi: (1) Wema; (2) utawa wa daraja ya juu; (3) mwenendo ulio bora. Aya hii inataka kusema hivi, ingawa Allah Hutoa ujira sawasawa, na Anajua kila kitu anachotoa mtu katika njia Yake, lakini wema wa daraja ya juu unaokubalika sana Kwake mtu anaweza kuufikia kwa kutoa vitu vya kila namna ambavyo anavipenda zaidi, maana kutoa kwa namna hii kunamfanya mtu ajinyime sana.

Inasimuliwa katika Hadithi ya kwamba Aya hii ilipoteremshwa, sahaba mmoja wa Mtume *s.a.w.* aitwaye Abu Talha, alisimama akamwambia, "Ee Mjumbe wa Mungu, bustani yangu inayoitwa Bi'r Rauhaa (iliyokuwa inaelekeana na Msikiti wa Madina) ndiyo mali yangu ninayoipenda mno, na sasa ninaitoa sadaka" (Bukhari, sura *Tafsiri*). Jambo hili linaonyesha jinsi watu walioingia Uislamu zamani walivyofanya bidii kutenda wema wa juu kabisa, kama ilivyokuwa ikiwaamuru Qur'an.

97. Kwa yakini Nyumba ya kwanza iliyowekwa kwa ajili ya watu ni ile iliyoko Bakka, yenye baraka na mwongozo kwa ajili ya walimwengu.

98. Humo mna Ishara zilizo wazi: mahali aliposimama Ibrahimu; na atakayeingia atakuwa salama. Na kwa ajili ya Allah watu wafanye Haji kwenye Nyumba hiyo awezaye kufunga safari kwenda huko; lakini aliyekufuru basi Allah si mhitaji kwa walimwengu.

99. Sema: Enyi watu wa Kitabu, kwa nini mnazikataa Ishara za Allah, hali Allah ni shahidi juu ya yale mnayoyatenda?

100. Sema: Enyi watu wa Kitabu, mbona mnamzuilia njia ya Allah yule aliyeamini mkitafuta kuipotoa na hali mnashuhudia? Na Allah si Mwenye kughafilika na yale mnayoyatenda.

إِنَّ أَوَّلَ بَيْتٍ وُّضِعَ لِلنَّاسِ لَلَّذِي بِبَكَّةَ
مُبٰرَكًا وَّهُدًى لِّلْعٰلَمِيْنَ ﴿٩٧﴾
فِيْهِ اٰيٰتٌۢ بَيِّنٰتٌ مَّقَامُ اِبْرٰهِيْمَ ۚ
وَمَنْ دَخَلَهٗ كَانَ اٰمِنًا ۗ وَلِلّٰهِ عَلَى النَّاسِ
حِجُّ الْبَيْتِ مَنِ اسْتَطَاعَ اِلَيْهِ سَبِيْلًا ۗ
وَمَنْ كَفَرَ فَاِنَّ اللّٰهَ غَنِيٌّ عَنِ الْعٰلَمِيْنَ ﴿٩٨﴾
قُلْ يٰٓاَهْلَ الْكِتٰبِ لِمَ تَكْفُرُوْنَ بِاٰيٰتِ
اللّٰهِ ۖ وَاللّٰهُ شَهِيْدٌ عَلٰى مَا تَعْمَلُوْنَ ﴿٩٩﴾
قُلْ يٰٓاَهْلَ الْكِتٰبِ لِمَ تَصُدُّوْنَ عَنْ
سَبِيْلِ اللّٰهِ مَنْ اٰمَنَ تَبْغُوْنَهَا عِوَجًا وَّاَنْتُمْ
شُهَدَآءُ ۗ وَمَا اللّٰهُ بِغَافِلٍ عَمَّا تَعْمَلُوْنَ ﴿١٠٠﴾

Aya 97. *Bakka* ni jina la bonde la Makka. Nyumba ya kwanza iliyosemwa hapa ni kaaba. Waandishi mashuhuri wa historia wanakiri ya kuwa hii ni nyumba ya zamani sana; hata hawakuweza kujua ni lini ilianza. (Tazama, Translation by C. M. Olderfather, London, 1935, Book III ch. 42 vol. ii, pp. 211 - 213. Muir, p. ciii. Rodwel chini ya sura 2:128).

Aya 98. *Watu wafanye Haji.* Kusudi la kufanya ibada ya Haji ni kuwazoeza watu kuacha majumba yao na makwao na kutengana na jamaa zao kwa ajili ya Allah. Pia Haji ni alama ya heshima inayopewa mahali ambapo mapendeleo ya Allah yalifanyika. Inawakumbusha waaminio safari ndefu ya kutaabisha aliyosafiri Ibrahimu na mwanawe, Ismaili, na mkewe, Hajira, ili akawaache hapo ili atimize mapendeleo ya Allah. Imani ya mahaji inazidi wanapoona jinsi Allah Alivyodumisha ukumbusho wa watu waliojitupa Kwake.

Zaidi ya hayo, Haji inawafanya Waislamu wa nchi mbalimbali kukutana mara moja kila mwaka kubadilishana maono na kufungamana katika urafiki na mapenzi. Pia tazama sura 2:197.

Aya 100. *Tabghuunahaa 'iwajan,* "Mkitafuta kuipotoa;" maneno haya pia yanaweza kutafsiriwa, "Mkitafuta upotofu ndani yake," yaani mnatamani utokee upotofu katika Uislamu; au mnatamani kupindua ukweli wa dini hii uonekane kwa sura nyingine isiyokuwa yake, na kugeuza mafundisho yake.

101. Enyi mlioamini, kama mkiwatii jamii ya wale waliopewa Kitabu, watakurudisheni kuwa makafiri baada ya imani yenu.

يٰٓاَيُّهَا الَّذِيْنَ اٰمَنُوْٓا اِنْ تُطِيْعُوْا فَرِيْقًا مِّنَ الَّذِيْنَ اُوْتُوا الْكِتٰبَ يَرُدُّوْكُمْ بَعْدَ اِيْمَانِكُمْ كٰفِرِيْنَ ﴿١٠١﴾

102. Na mtakataaje hali ninyi mnasomewa Aya za Allah, na Mtume Wake yumo kati yenu? Na mwenye kumshika Allah sawasawa, basi yeye amekwisha ongozwa kwenye njia iliyonyooka.

وَكَيْفَ تَكْفُرُوْنَ وَاَنْتُمْ تُتْلٰى عَلَيْكُمْ اٰيٰتُ اللّٰهِ وَفِيْكُمْ رَسُوْلُهٗ ؕ وَمَنْ يَّعْتَصِمْ بِاللّٰهِ فَقَدْ هُدِيَ اِلٰى صِرَاطٍ مُّسْتَقِيْمٍ ﴿١٠٢﴾

FUNGU 11

103. Enyi mlioamini, Mcheni Allah ipasavyo kumcha; wala msife ila mmekwisha kuwa wanyenyekevu kamili.

يٰٓاَيُّهَا الَّذِيْنَ اٰمَنُوا اتَّقُوا اللّٰهَ حَقَّ تُقٰتِهٖ وَلَا تَمُوْتُنَّ اِلَّا وَاَنْتُمْ مُّسْلِمُوْنَ ﴿١٠٣﴾

104. Na shikeni kamba ya Allah nyote, wala msiachane; na kumbukeni neema ya Allah iliyo juu yenu mlipoku wa maadui naye Akaziunganisha nyoyo zenu, hivyo kwa neema yake mkawa ndugu; na mlikuwa ukingoni mwa shimo la moto naye Akawaokoeni nalo. Hivyo ndivyo Allah Anavyokubainishieni Aya Zake ili mpate kuongoka.

وَاعْتَصِمُوْا بِحَبْلِ اللّٰهِ جَمِيْعًا وَّلَا تَفَرَّقُوْا ۠ وَاذْكُرُوْا نِعْمَتَ اللّٰهِ عَلَيْكُمْ اِذْ كُنْتُمْ اَعْدَآءً فَاَلَّفَ بَيْنَ قُلُوْبِكُمْ فَاَصْبَحْتُمْ بِنِعْمَتِهٖٓ اِخْوَانًا ۚ وَكُنْتُمْ عَلٰى شَفَا حُفْرَةٍ مِّنَ النَّارِ فَاَنْقَذَكُمْ مِّنْهَا ؕ كَذٰلِكَ يُبَيِّنُ اللّٰهُ لَكُمْ اٰيٰتِهٖ لَعَلَّكُمْ تَهْتَدُوْنَ ﴿١٠٤﴾

Aya 102. *Mwenye kumshika Allah.* Maneno haya yana maana mbili: (1) Mtu aliyejihifadhi na kutenda madhambi akifuata amri za Mwenyezi Mungu; (2) Mtu anayejiunganisha na Allah na anashikilia kwa uhodari, na kwa hivyo anajipatia njia ya kuendelea na kukua.

Aya 104. *Hablil-Laah,* "Kamba ya Allah." Mtume *s.a.w.* alisema, "Kitabu cha Allah ni kamba ya Mungu iliyonyooshwa toka mbinguni mpaka ardhini" (Jarir, Jalada 4 uk. 30). Kwa maana iliyo pana zaidi "Kamba ya Allah" ambayo Waislamu wakiishika watakaa katika hali ya umoja ni (1) Qur'an; (2) Mjumbe wa Mungu (3) Makhalifa wa Mjumbe wa Mungu. Katika Aya hii wanaonywa Waislamu wasifarikiane, maana kufarikiana ni jambo la hatari kwao.

وَلْتَكُنْ مِّنْكُمْ اُمَّةٌ يَّدْعُوْنَ اِلَى الْخَيْرِ
وَيَاْمُرُوْنَ بِالْمَعْرُوْفِ وَيَنْهَوْنَ عَنِ
الْمُنْكَرِ ؕ وَاُولٰٓئِكَ هُمُ الْمُفْلِحُوْنَ ﴿١٠٥﴾

105. Na liwepo miongoni mwenu kundi linaloita kwenye kheri na kuamuru kutenda mema na kukataza maovu, na hao ndiyo wenye kufaulu.

وَلَا تَكُوْنُوْا كَالَّذِيْنَ تَفَرَّقُوْا وَاخْتَلَفُوْا
مِنْۢ بَعْدِ مَا جَآءَهُمُ الْبَيِّنٰتُ ؕ وَاُولٰٓئِكَ
لَهُمْ عَذَابٌ عَظِيْمٌ ۙ﴿١٠٦﴾

106. Wala msiwe kama wale waliofarakana na kuhitilafiana baada ya kuwafikia dalili zilizo wazi; na hao ndiyo watakaokuwa na adhabu kubwa.

يَّوْمَ تَبْيَضُّ وُجُوْهٌ وَّتَسْوَدُّ وُجُوْهٌ ۚ
فَاَمَّا الَّذِيْنَ اسْوَدَّتْ وُجُوْهُهُمْ ۫
اَكَفَرْتُمْ بَعْدَ اِيْمَانِكُمْ فَذُوْقُوا
الْعَذَابَ بِمَا كُنْتُمْ تَكْفُرُوْنَ ﴿١٠٧﴾

107. Siku ambayo nyuso zitakuwa nyeupe, na nyuso (nyingine) zitakuwa nyeusi. Waama hao nyuso zao zitakazokuwa nyeusi (wataambiwa): Je, mlikufuru baada ya imani yenu? Basi onjeni adhabu kwa sababu mlikuwa mkikataa.

وَاَمَّا الَّذِيْنَ ابْيَضَّتْ وُجُوْهُهُمْ فَفِيْ
رَحْمَةِ اللّٰهِ ؕ هُمْ فِيْهَا خٰلِدُوْنَ ﴿١٠٨﴾

108. Waama hao nyuso zao zitakazokuwa nyeupe, basi watakuwa katika rehema ya Allah. Wao humo watakaa milele.

تِلْكَ اٰيٰتُ اللّٰهِ نَتْلُوْهَا عَلَيْكَ بِالْحَقِّ ؕ وَمَا
اللّٰهُ يُرِيْدُ ظُلْمًا لِّلْعٰلَمِيْنَ ﴿١٠٩﴾

109. Hizi ni Aya za Allah Tunazokusomea kwa haki; na Allah Hataki dhuluma kwa walimwengu.

وَلِلّٰهِ مَا فِي السَّمٰوٰتِ وَمَا فِي الْاَرْضِ ؕ
وَاِلَى اللّٰهِ تُرْجَعُ الْاُمُوْرُ ﴿١١٠﴾ ع ١١

110. Na kila kilichomo mbinguni na kilichomo ardhini ni cha Allah; na mambo yote hurudishwa kwa Allah.

Aya 105. Siyo maana ya Aya hii kuwa kazi ya kuhubiri dini iwe kwa ajili ya watu wachache tu, la. Bali mradi wake ni kuwa wote wajaribu kuhubiri na kueneza Uislamu, na pia kuwe kundi maalumu lisilo na kazi nyingine isipokuwa hiyo tu.

Aya 107. *Nyeupe,* yaani "furaha" na *nyeusi,* "huzuni," ndizo maana zinazoelezwa na Qur'an yenyewe (tazama sura 3:108 na 16:59 na pia linganisha na sura 75:23 na 80:39-40).

FUNGU 12

كُنْتُمْ خَيْرَ اُمَّةٍ اُخْرِجَتْ لِلنَّاسِ
تَاْمُرُوْنَ بِالْمَعْرُوْفِ وَتَنْهَوْنَ عَنِ
الْمُنْكَرِ وَتُؤْمِنُوْنَ بِاللّٰهِ ؕ وَلَوْ اٰمَنَ اَهْلُ
الْكِتٰبِ لَكَانَ خَيْرًا لَّهُمْ ؕ مِنْهُمُ
الْمُؤْمِنُوْنَ وَ اَكْثَرُهُمُ الْفٰسِقُوْنَ ﴿۱۱۰﴾

111. Ninyi ni umati bora mliotolewa kwa ajili ya manufaa ya watu wote, mnaamuru yaliyo mema na mnakataza maovu, na mnamwamini Allah. Na kama watu wa Kitabu wangaliamini ingalikuwa bora kwao; kati yao wako waaminio, lakini wengi wao ni wavunjao amri.

لَنْ يَّضُرُّوْكُمْ اِلَّاۤ اَذًى ؕ وَ اِنْ
يُّقَاتِلُوْكُمْ يُوَلُّوْكُمُ الْاَدْبَارَ ۫ ثُمَّ
لَا يُنْصَرُوْنَ ﴿۱۱۱﴾

112. Hawatawadhuruni kamwe ila udhia kidogo tu; na kama watapigana nanyi watawapeni migongo, kisha hawatasaidiwa.

ضُرِبَتْ عَلَيْهِمُ الذِّلَّةُ اَيْنَ مَا ثُقِفُوْۤا اِلَّا
بِحَبْلٍ مِّنَ اللّٰهِ وَحَبْلٍ مِّنَ النَّاسِ وَبَآءُوْ
بِغَضَبٍ مِّنَ اللّٰهِ وَ ضُرِبَتْ عَلَيْهِمُ
الْمَسْكَنَةُ ؕ ذٰلِكَ بِاَنَّهُمْ كَانُوْا يَكْفُرُوْنَ
بِاٰيٰتِ اللّٰهِ وَ يَقْتُلُوْنَ الْاَنْۢبِيَآءَ بِغَيْرِ حَقٍّ ؕ
ذٰلِكَ بِمَا عَصَوْا وَّ كَانُوْا يَعْتَدُوْنَ ﴿۱۱۲﴾

113. Wamepigwa dhila mahali po pote wanapopatikana ila kwa (kushika) kamba ya Allah na kamba ya watu. Nao wamerudi na hasira ya Allah, na umaskini umepigwa juu yao. Hii ni kwa sababu ya wao kutoamini Ishara za Allah, na kuwapinga mno Manabii bila ya haki; hayo ni kwa sababu waliasi na walikuwa wakiruka mipaka.

لَيْسُوْا سَوَآءً ؕ مِنْ اَهْلِ الْكِتٰبِ اُمَّةٌ
قَآئِمَةٌ يَّتْلُوْنَ اٰيٰتِ اللّٰهِ اٰنَآءَ الَّيْلِ وَهُمْ
يَسْجُدُوْنَ ﴿۱۱۳﴾

114. Wao wote si sawa. Miongoni mwa watu wa Kitabu lipo kundi la watu wanaosimama imara katika msimamo wao; wanasoma Aya za Allah nyakati za usiku na huku wakisujudu.

يُؤْمِنُوْنَ بِاللّٰهِ وَالْيَوْمِ الْاٰخِرِ وَيَاْمُرُوْنَ
بِالْمَعْرُوْفِ وَيَنْهَوْنَ عَنِ الْمُنْكَرِ
وَيُسَارِعُوْنَ فِى الْخَيْرٰتِ ؕ وَ اُولٰٓئِكَ مِنَ
الصّٰلِحِيْنَ ﴿۱۱۴﴾

115. Wanamwamini Allah na siku ya Mwisho na wanaamrisha mema na wanakataza maovu na wanaharakia mambo mema; na hao ndiyo miongoni mwa watendao mema.

Aya 111. Ubora wa Waislamu unategemea sharti zilizoelezwa, yaani wawe wenye kuuhubiri Uislamu kwa walimwengu, wawe wenye kuamrisha wema na kukataza uovu. Kujigamba tu kwa mdomo kuwa mtu ni Mwislamu hakumpi ubora wo wote. Na kwa kuhubiri dini Allah amesema, *Uite (watu) kwenye njia ya Mola wako kwa hekima na mauidha mema, na ushindane nao kwa namna iliyo bora* (sura 16:126).

Aya 113. *Kamba ya Allah* ni dini ya Kiislamu, na kamba ya watu ni dola za wasio Waislamu.

وَمَا يَفْعَلُوْا مِنْ خَيْرٍ فَلَنْ يُّكْفَرُوْهُ ؕ
وَاللّٰهُ عَلِيْمٌۢ بِالْمُتَّقِيْنَ ﴿۱۱۶﴾

116. Na heri yo yote watakayoifanya hawataikataliwa; na Allah Anawajua vyema wamchao.

اِنَّ الَّذِيْنَ كَفَرُوْا لَنْ تُغْنِيَ عَنْهُمْ
اَمْوَالُهُمْ وَلَاۤ اَوْلَادُهُمْ مِّنَ اللّٰهِ شَيْـًٔا ؕ
وَاُولٰٓئِكَ اَصْحٰبُ النَّارِ ۚ هُمْ فِيْهَا
خٰلِدُوْنَ ﴿۱۱۷﴾

117. Hakika wale waliokufuru, hazitawafaa mali zao wala watoto wao hata kidogo mbele ya Allah; na hao ndiyo watu wa Motoni; watakaa humo kwa muda mrefu sana.

مَثَلُ مَا يُنْفِقُوْنَ فِيْ هٰذِهِ الْحَيٰوةِ الدُّنْيَا
كَمَثَلِ رِيْحٍ فِيْهَا صِرٌّ اَصَابَتْ حَرْثَ
قَوْمٍ ظَلَمُوْۤا اَنْفُسَهُمْ فَاَهْلَكَتْهُ ؕ وَمَا
ظَلَمَهُمُ اللّٰهُ وَلٰكِنْ اَنْفُسَهُمْ يَظْلِمُوْنَ ﴿۱۱۸﴾

118. Mfano wa vile wanavyovitoa katika maisha haya ya dunia ni kama upepo ambao ndani yake mna baridi kali; ukalisibu shamba la watu waliozidhulumu nafsi zao na ukaliangamiza; na Allah hakuwadhulumu, bali wao wenyewe wanadhulumu nafsi zao.

يٰۤاَيُّهَا الَّذِيْنَ اٰمَنُوْا لَا تَتَّخِذُوْا بِطَانَةً
مِّنْ دُوْنِكُمْ لَا يَاْلُوْنَكُمْ خَبَالًا ؕ وَدُّوْا مَا
عَنِتُّمْ ۚ قَدْ بَدَتِ الْبَغْضَآءُ مِنْ
اَفْوَاهِهِمْ ۖۚ وَمَا تُخْفِيْ صُدُوْرُهُمْ اَكْبَرُ ؕ
قَدْ بَيَّنَّا لَكُمُ الْاٰيٰتِ اِنْ كُنْتُمْ تَعْقِلُوْنَ ﴿۱۱۹﴾

119. Enyi mlioamini, msimfanye mtu kuwa msiri wenu asiyekuwa katika ninyi: hao hawatakosa kuwatieni hasara; wanayapenda yale yanayowadhuruni; bila shaka bughudha imedhihirika katika midomo yao, na yanayoficha vifua vyao ni makubwa zaidi; kwa yakini tumewabainishieni dalili ikiwa ninyi mnafahamu.

هٰۤاَنْتُمْ اُولَآءِ تُحِبُّوْنَهُمْ وَلَا يُحِبُّوْنَكُمْ
وَتُؤْمِنُوْنَ بِالْكِتٰبِ كُلِّهٖ ۚ وَاِذَا لَقُوْكُمْ
قَالُوْۤا اٰمَنَّا ۖۚ وَاِذَا خَلَوْا عَضُّوْا عَلَيْكُمُ
الْاَنَامِلَ مِنَ الْغَيْظِ ؕ قُلْ مُوْتُوْا بِغَيْظِكُمْ ؕ
اِنَّ اللّٰهَ عَلِيْمٌۢ بِذَاتِ الصُّدُوْرِ ﴿۱۲۰﴾

120. Lo! Ninyi ndiyo hao mnaowapenda hali wao hawawapendeni, nanyi mnaamini Kitabu chote; na wanapokutana nanyi husema, Tumeamini, lakini wanapokuwa peke yao, wanakuumieni nyanda kwa ajili ya ghadhabu. Sema: Kufeni kwa ghadhabu yenu; hakika Allah Anayajua yaliyomo vifuani.

Aya 118. Aya hii inaonyesha ya kwamba juhudi wanazotumia wasioamini ili kuudhuru Uislamu zitawapindukia wenyewe. Cho chote wanachofanya na cho chote wanachotoa ili kuujeruhi Uislamu kitawajeruhi wenyewe. Allah ameleta Uislamu kwa ajili ya faida yao wenyewe, lakini wakiukataa watajiletea maangamizo.

إِنْ تَمْسَسْكُمْ حَسَنَةٌ تَسُؤْهُمْ ۖ وَإِنْ تُصِبْكُمْ سَيِّئَةٌ يَفْرَحُوا بِهَا ۖ وَإِنْ تَصْبِرُوا وَتَتَّقُوا لَا يَضُرُّكُمْ كَيْدُهُمْ شَيْئًا ۗ إِنَّ اللَّهَ بِمَا يَعْمَلُونَ مُحِيطٌ ﴿١٢٠﴾ ع ١٢

121. Kama ukiwafikieni wema unawakera, na kama likiwapateni baya wanalifurahia; na kama ninyi mkisubiri na kumcha Allah, hila zao hazitakudhuruni kitu. Hakika Allah Anayazunguka wanayoyatenda.

FUNGU 13

وَإِذْ غَدَوْتَ مِنْ أَهْلِكَ تُبَوِّئُ الْمُؤْمِنِينَ مَقَاعِدَ لِلْقِتَالِ ۗ وَاللَّهُ سَمِيعٌ عَلِيمٌ ﴿١٢١﴾

122. Na (kumbuka) ulipotoka asubuhi kutoka kwa ahali zako kuwapangia waaminio mahali pa kupigana; na Allah ndiye Asikiaye, Ajuaye.

إِذْ هَمَّتْ طَّائِفَتَانِ مِنْكُمْ أَنْ تَفْشَلَا ۙ وَاللَّهُ وَلِيُّهُمَا ۗ وَعَلَى اللَّهِ فَلْيَتَوَكَّلِ الْمُؤْمِنُونَ ﴿١٢٢﴾

123. (Kumbuka) makundi mawili miongoni mwenu yalipodhamiria kuonyesha woga na hali Allah Alikuwa mlinzi wa yote mawili; na waaminio wanapaswa kumtegemea Allah.

Aya 122. Aya hii inaeleza habari za vita vya Uhud vilivyopiganwa katika mwaka wa tatu wa Hijra. Makureishi waliposhindwa katika vita vya Badri, walianza tena kujiandaa vyema ili kuleta shambulio jingine Madina, na wakaenda na jeshi lenye watu 3,000 ambalo lilipambana na jeshi la Mtume *s.a.w.* lenye watu 700 mahali panapoitwa Uhud. Kwanza Makureishi walihemewa wakaanza kukimbia. Waislamu 50 wenye mishale waliokuwa wamewekwa mahali kilimani wakiambiwa wasiondoke hapo ingawa itokee nini, walipoona adui anakimbia, wakaondoka pale kuwafuata wenzao. Maadui walipoona kilimani kuwazi wakazungukiako na wakawatokea kwa nyuma. Hapo Waislamu wakapigwa vibaya na kushindwa, na Mtume *s.a.w.* akajeruhiwa sana.

Aya 123. *Makundi mawili* ni Banu Salma na Banu Haaritha wa makabila ya Aus na Khazraj wa Madina.

Juu ya Allah wategemee waaminio. Maneno haya si mradi wake ya kwamba Mwislamu aache kujishughulisha na njia kufanya kazi za kupatia anavyovitaka, na akalie kumwomba Mungu akingojea msaada Wake. Hii si maana ya kutawakali kwa Allah, na haijulikani katika mafundisho ya Kiislamu. Islam inafundisha ya kwamba mumini wa kweli atumie kila njia ya kupatia anachokitaka na papo asitegemee njia hizo, bali amtegemee Allah peke yake akiona njia hizo kwamba zitafanikiwa ikiwa Mungu atapenda. Mtume *s.a.w.* alisema, "Funga goti la ngamia wako kisha umtegemee Allah" kumwambia mtu mmoja ambaye aliacha kumfunga ngamia wake akisema, amemtegemea Allah kuwa atamlinda.

وَلَقَدْ نَصَرَكُمُ اللّٰهُ بِبَدْرٍ وَّاَنْتُمْ اَذِلَّةٌ ۚ فَاتَّقُوا اللّٰهَ لَعَلَّكُمْ تَشْكُرُوْنَ ﴿١٢٣﴾

124. Na bila shaka Allah Aliwasaidieni katika (vita vya) Badri hali ninyi mlikuwa dhaifu. Basi mcheni Allah ili mpate kushukuru.

اِذْ تَقُوْلُ لِلْمُؤْمِنِيْنَ اَلَنْ يَّكْفِيَكُمْ اَنْ يُّمِدَّكُمْ رَبُّكُمْ بِثَلٰثَةِ اٰلٰفٍ مِّنَ الْمَلٰٓئِكَةِ مُنْزَلِيْنَ ﴿١٢٤﴾

125. Ulipowaambia waaminio. Je, haitawatosheni kwamba Mola wenu Awasaidieni kwa Malaika elfu tatu watakaoteremshwa?

بَلٰٓى ۙ اِنْ تَصْبِرُوْا وَتَتَّقُوْا وَيَاْتُوْكُمْ مِّنْ فَوْرِهِمْ هٰذَا يُمْدِدْكُمْ رَبُّكُمْ بِخَمْسَةِ اٰلٰفٍ مِّنَ الْمَلٰٓئِكَةِ مُسَوِّمِيْنَ ﴿١٢٥﴾

126. Naam! kama mkisubiri na kujilinda na watakufikieni haraka kwa kishindo, hapo Mola wenu Atawasaidieni kwa Malaika elfu tano washambuliao kwa nguvu.

Aya 124. *Badri* ni jina la mahali njiani katikati ya Makka na Madina. Mahali hapo pamepata jina hilo kutoka chemchem ya mtu mmoja aliyeitwa Badri. Vita ya Badri inayosemwa hapa ilipiganwa karibu na mahali hapa.

Maneno ya Aya hii wanaambiwa Waislamu, na Mtume aliyatumia baada ya vita vya Uhud. Yanawakumbusha Waislamu ya kwamba Allah aliwapa ushindi katika vita vya Badri hali walikuwa dhaifu zaidi kuliko walivyokuwa katika mapigano ya Uhud kwa sababu walitii, wakasubiri na kumcha Mungu. Hivyo kushindwa kwao vita Uhud ni kwa sababu kutotii kwa wenzao, ingawa hawakukusudia kuasi amri waliyopewa na Mtume s.a.w. Na inaonekana wanaahidiwa msaada baadaye ikiwa watatubu kosa lao.

Aya 125. Aya hii inaeleza ya kwamba ikiwa watu wa Makka watawashambulia tena Waislamu baadaye baada ya vita hivi vya Uhud, basi Allah atawasaidia Waislamu kwa kuwateremshia Malaika elfu tatu. Aya hii haihusu vita vya Badri vilivyotajwa katika Aya iliyotangulia kwa namna ya kutaka kuunganisha habari hiyo na hii, maana hesabu ya Malaika waliopelekwa kuwasaidia Waislamu katika vita vya Badri tusomavyo katika sura 8:10 ni elfu moja, si elfu tatu kama waliotajwa hapa. Kutimizwa kwa ahadi hii inayotajwa kunaelezwa katika sura hii Aya 152.

Aya 126. Aya hii inaonyesha ya kwamba, kama makafiri wangerudi kuwashambulia kwa haraka, Allah Angewasaidia Waislamu kwa Malaika elfu tano. Tofauti ya hesabu hii ya Malaika wanaotajwa katika Aya hii na Aya ya kabla yake, imekuja kwa sababu ya tofauti katika hali ya Waislamu. Baada ya vita vya Uhud, Waislamu walikuwa wamechoka sana na wenye majeraha na hivyo walihitaji msaada zaidi kuliko ambavyo wangehitaji, kama adui angalikawia.

Kwa hakika maadui zao walifikiria kuwarudia, lakini Allah akawazuia. Kwa kifupi ilikuwa hivi: Makureishi walipokuwa wakirudi Makka baada ya vita vya Uhud, Waarabu waliokuwa katika vitongoji vya Madina waliwauliza vita vimekuwaje. Wakawajibu kuwa wao ndio walioshinda Wale Waarabu wakawafedhehesha kwa kuwaambia, "Kama kweli mmeshinda, mateka wako wapi? Mmeleta nini kutoka vitani?" Kebehi hii ikawauma sana Makureishi, wakafunga nia warejee mara hiyo kuwashambulia Waislamu ili wapate kuwa na uso mbele za watu. Mtume s.a.w. alipojua habari hii, siku ya pili baada ya vita vya Uhud akatoa amri Waislamu

وَمَا جَعَلَهُ اللّٰهُ اِلَّا بُشْرٰى لَكُمْ وَلِتَطْمَئِنَّ قُلُوْبُكُمْ بِهٖ ۚ وَمَا النَّصْرُ اِلَّا مِنْ عِنْدِ اللّٰهِ الْعَزِيْزِ الْحَكِيْمِ ﴿١٢٧﴾

127. Na Allah Hakufanya (ahadi) hii ila iwe bishara kwenu, na ili mioyo yenu ipate kutulia kwayo; na msaada hautoki isipokuwa kwa Allah, Mwenye ushindi kamili, Mwenye hekima;

لِيَقْطَعَ طَرَفًا مِّنَ الَّذِيْنَ كَفَرُوْٓا اَوْ يَكْبِتَهُمْ فَيَنْقَلِبُوْا خَآئِبِيْنَ ﴿١٢٨﴾

128. Ili Akate sehemu katika wale waliokufuru au kuwadhalilisha ili wapate kurudi hali wameshindwa.

لَيْسَ لَكَ مِنَ الْاَمْرِ شَيْءٌ اَوْ يَتُوْبَ عَلَيْهِمْ اَوْ يُعَذِّبَهُمْ فَاِنَّهُمْ ظٰلِمُوْنَ ﴿١٢٩﴾

129. Wewe huna mamlaka yoyote, kama (Allah) Awaonee huruma au awaadhibu, wao kwa vyovyote vile ni wadhalimu tu.

وَلِلّٰهِ مَا فِى السَّمٰوٰتِ وَمَا فِى الْاَرْضِ ۚ يَغْفِرُ لِمَنْ يَّشَآءُ وَيُعَذِّبُ مَنْ يَّشَآءُ ۚ وَاللّٰهُ غَفُوْرٌ رَّحِيْمٌ ﴿١٣٠﴾ ع ١٣ ٩ ٤

130. Na ni vya Allah vilivyomo mbinguni na vilivyomo ardhini; Humsamehe Amtakaye na Humwadhibu Amtakaye, na Allah ni Msamehevu, Mrehemevu.

FUNGU 14

يٰٓاَيُّهَا الَّذِيْنَ اٰمَنُوْا لَا تَاْكُلُوا الرِّبٰٓوا اَضْعَافًا مُّضٰعَفَةً ۠ وَّاتَّقُوا اللّٰهَ لَعَلَّكُمْ تُفْلِحُوْنَ ﴿١٣١﴾ ع

131. Enyi mlioamini, msile riba (juu ya mali yenu) inayoizidisha (mali) maradufu; na Mcheni Allah ili mpate kustawi.

وَاتَّقُوا النَّارَ الَّتِىْٓ اُعِدَّتْ لِلْكٰفِرِيْنَ ﴿١٣٢﴾ ع

132. Na ogopeni Moto ambao umeandaliwa makafiri.

وَاَطِيْعُوا اللّٰهَ وَالرَّسُوْلَ لَعَلَّكُمْ تُرْحَمُوْنَ ﴿١٣٣﴾ ع

133. Na Mtiini Allah na Mtume ili mpate kurehemewa.

---

waliokuwa katika vita vya Uhud waondoke kuwafuatia Makureishi. Waislamu wakaenda hadi Hamraa'l-Asad, mahali penye umbali wa maili nane kutoka Madina. Kushtukizwa huku kukawatia kiwewe Makureishi kuona Waislamu walivyo hodari. Wakawa hawana budi ila kukimbia na kurudi Makka. Ilitokea hivyo kwa sababu Malaika walitia hofu mioyoni mwao. Kama si hivyo hawakuwa na sababu ya kumkimbia adui waliyemtia hasara nzito sana jana yake, hali hesabu ya adui huyo imekwisha pungua kabisa na bado ana majeraha mabichi yanayomwuma.

Aya 131. Riba ya kila namna imekatazwa. Kuna watu wanaosema ya kuwa siku hizi biashara haiwezi kuendelea bila riba. Hii si kweli, kwani Waislamu walitawala milki kubwa kubwa na walifanikisha biashra kubwa kubwa pasipo kutoa wala kupokea riba.

وَسَارِعُوْٓا اِلٰى مَغْفِرَةٍ مِّنْ رَّبِّكُمْ وَجَنَّةٍ
عَرْضُهَا السَّمٰوٰتُ وَالْاَرْضُ ۙ اُعِدَّتْ
لِلْمُتَّقِيْنَ ﴿١٣٣﴾

134. Na harakieni kuomba msamaha kwa Mola wenu na Pepo ambayo upana wake ni (sawa na) mbingu na ardhi, iliyoandaliwa kwa ajili ya wamchao.

الَّذِيْنَ يُنْفِقُوْنَ فِي السَّرَّآءِ وَالضَّرَّآءِ
وَالْكٰظِمِيْنَ الْغَيْظَ وَالْعَافِيْنَ عَنِ
النَّاسِ ؕ وَاللّٰهُ يُحِبُّ الْمُحْسِنِيْنَ ﴿١٣٤﴾

135. Ambao hutoa katika (hali ya) faraja na dhiki, na wazuiao ghadhabu na kuwasamehe watu; na Allah Huwapenda wafanyao ihsani.

وَالَّذِيْنَ اِذَا فَعَلُوْا فَاحِشَةً اَوْ ظَلَمُوْٓا
اَنْفُسَهُمْ ذَكَرُوا اللّٰهَ فَاسْتَغْفَرُوْا
لِذُنُوْبِهِمْ ۫ وَمَنْ يَّغْفِرُ الذُّنُوْبَ اِلَّا
اللّٰهُ ۖ وَلَمْ يُصِرُّوْا عَلٰى مَا فَعَلُوْا
وَهُمْ يَعْلَمُوْنَ ﴿١٣٥﴾

136. Na ambao wanapofanya ubaya au kudhulumu nafsi zao humkumbuka Allah na kuomba msamaha kwa dhambi zao, na nani anayeghofiri dhambi isipokuwa Allah? na hawaendelei na (maovu) waliyoyafanya hali wanajua.

اُولٰٓئِكَ جَزَآؤُهُمْ مَّغْفِرَةٌ مِّنْ رَّبِّهِمْ
وَجَنّٰتٌ تَجْرِيْ مِنْ تَحْتِهَا الْاَنْهٰرُ
خٰلِدِيْنَ فِيْهَا ؕ وَنِعْمَ اَجْرُ الْعٰمِلِيْنَ ﴿١٣٦﴾

137. Hao ndiyo malipo yao yatakuwa msamaha kwa Mola wao na Bustani zipitazo mito ndani yake ambamo watakaa milele. Na ni mzuri ulioje ujira wa watendao (mema)!.

قَدْ خَلَتْ مِنْ قَبْلِكُمْ سُنَنٌ ۙ فَسِيْرُوْا فِي
الْاَرْضِ فَانْظُرُوْا كَيْفَ كَانَ عَاقِبَةُ
الْمُكَذِّبِيْنَ ﴿١٣٧﴾

138. Bila shaka zimepita desturi nyingi kabla yenu, basi safirini ardhini na mwone ulikuwaje mwisho wa wale waliokadhibisha.

هٰذَا بَيَانٌ لِّلنَّاسِ وَهُدًى وَّمَوْعِظَةٌ
لِّلْمُتَّقِيْنَ ﴿١٣٨﴾

139. Hili ni tangazo lililo wazi kwa watu, na ni mwongozo na mawaidha kwa wacha Mungu.

وَلَا تَهِنُوْا وَلَا تَحْزَنُوْا وَاَنْتُمُ
الْاَعْلَوْنَ اِنْ كُنْتُمْ مُّؤْمِنِيْنَ ﴿١٣٩﴾

140. Na msilegee wala msihuzunike maana ninyi ndio wenye kushinda kama mu waaminio.

اِنْ يَّمْسَسْكُمْ قَرْحٌ فَقَدْ مَسَّ الْقَوْمَ
قَرْحٌ مِّثْلُهٗ ؕ وَتِلْكَ الْاَيَّامُ نُدَاوِلُهَا بَيْنَ
النَّاسِ ۚ وَلِيَعْلَمَ اللّٰهُ الَّذِيْنَ اٰمَنُوْا
وَيَتَّخِذَ مِنْكُمْ شُهَدَآءَ ؕ وَاللّٰهُ لَا يُحِبُّ
الظّٰلِمِيْنَ ﴿١٤٠﴾

141. Kama mmepata jeraha, basi watu wamekwisha pata jeraha kama hilo, na hizo ndizo zile siku Tunazowabadilishia watu kwa zamu, na ili Allah Apambanue walioamini na Afanye miongoni mwenu mashahidi, na Allah Hawapendi madhalimu.

142. Na ili Allah Awatakase walioamini na kuwafuta waliokufuru.

وَلِيُمَحِّصَ اللّٰهُ الَّذِيْنَ اٰمَنُوْا وَيَمْحَقَ الْكٰفِرِيْنَ ﴿١٤٢﴾

143. Je, mnadhani mtaingia Peponi na hali Allah Hajawapambanua wale waliofanya jihadi miongoni mwenu na kuwapambanua waliofanya subira?

اَمْ حَسِبْتُمْ اَنْ تَدْخُلُوا الْجَنَّةَ وَلَمَّا يَعْلَمِ اللّٰهُ الَّذِيْنَ جٰهَدُوْا مِنْكُمْ وَيَعْلَمَ الصّٰبِرِيْنَ ﴿١٤٣﴾

144. Na kwa yakini mlikuwa mkiyatamani mauti kabla ya kukutana nayo; sasa mmeyaona katika hali hii kwamba mmebaki mnakodoa tu macho.

وَلَقَدْ كُنْتُمْ تَمَنَّوْنَ الْمَوْتَ مِنْ قَبْلِ اَنْ تَلْقَوْهُ ۖ فَقَدْ رَاَيْتُمُوْهُ وَاَنْتُمْ تَنْظُرُوْنَ ﴿١٤٣﴾ ع ١٤

FUNGU 15

145. Na siye Muhammad ila yu Mtume. Bila shaka wamekwisha fariki kabla yake Mitume. Je, akifa au akiuawa mtarudi nyuma kwa visigino vyenu? Na Atakayerudi nyuma kwa visigino vyake hatamdhuru Allah cho chote; Na Allah bila shaka Atawalipa wanaoshukuru.

وَمَا مُحَمَّدٌ اِلَّا رَسُوْلٌ ۚ قَدْ خَلَتْ مِنْ قَبْلِهِ الرُّسُلُ ؕ اَفَاْئِنْ مَّاتَ اَوْ قُتِلَ انْقَلَبْتُمْ عَلٰٓى اَعْقَابِكُمْ ؕ وَمَنْ يَّنْقَلِبْ عَلٰى عَقِبَيْهِ فَلَنْ يَّضُرَّ اللّٰهَ شَيْـًٔا ؕ وَسَيَجْزِى اللّٰهُ الشّٰكِرِيْنَ ﴿١٤٥﴾

Aya 145. Katika vita vya Uhud, Waislamu walipoumizwa vibaya, ulienea uvumi kuwa Mtume *s.a.w.* ameuawa. Baadhi ya Waislamu walianza kubabaika. Allah Alishusha Aya hiyo isemayo kuwa Muhammad *s.a.w.* ni Mtume tu, akifa si neno, kwani Manabii waliomtangulia wamekwisha kufa. Hivyo waaminio hawana haja ya kutikisika imani zao, kwani Mungu wao ni hai, hafi, na Anaweza kuwasaidia daima.

Miaka saba baada ya tukio hili Mtume *s.a.w*. alifariki. Seyyidna Umar alisimama msikitini, upanga mkononi, akasema, "Mtu atakayesema kuwa Mtume wa Mungu amekufa, nitakata kichwa chake. Hakufa bali amekwenda kwa Mola wake (yaani amepanda mbinguni) kama vile Musa alivyokwenda kwa Mola wake, naye atarudi na kuwaadhibu wanafiki." Wakati huu Abubakar aliyekuwa hayupo Mtume alipofariki, alikuwa akija kwa haraka; akaingia katika chumba cha Mtume *s.a.w.* na alipoona kuwa kweli amefariki, akabusu paji la uso wake, akisema "u-mzuri katika mauti kama ulivyokuwa mzuri katika uhai bila shaka Allah hatakuletea vifo viwili." Kisha akatoka nje katika hali ya imara, akamwambia Umar akae chini, na akawaelekea masahaba waliokuwa wamekusanyika msikitini na akawasomea Aya hii, *Siye Muhammad ila yu Mtume, bila shaka wamekwisha fariki kabla yake Mitume, je, akifa au akiuawa mtarudi nyuma?* Seyyidna Umar na masahaba wengine kusikia Aya hii wakapoa kwa huzuni (Bukhari). Hivyo Aya hii upande mwengine inahakikisha ya kuwa Manabii waliokuwa kabla ya Mtume *s.a.w.* wamekwisha kufa, maana kama Musa na Isa au Mtume ye yote angekuwa hai isingesomwa Aya hii kuhakikisha kuwa Mtume *s.a.w.* amekufa.

وَمَا كَانَ لِنَفْسٍ اَنْ تَمُوْتَ اِلَّا بِاِذْنِ اللّٰهِ كِتٰبًا مُّؤَجَّلًا ؕ وَمَنْ يُّرِدْ ثَوَابَ الدُّنْيَا نُؤْتِهٖ مِنْهَا ۚ وَمَنْ يُّرِدْ ثَوَابَ الْاٰخِرَةِ نُؤْتِهٖ مِنْهَا ؕ وَسَنَجْزِى الشّٰكِرِيْنَ ﴿۱۴۵﴾

146. Na nafsi haiwezi kufa ila kwa amri ya Allah, ajali iliyowekwa. Na atakaye malipo ya dunia, Tunampa katika hayo; na atakaye malipo ya Akhera, Tutampa katika hayo; na kwa yakini Tutawalipa wanaoshukuru.

وَكَاَيِّنْ مِّنْ نَّبِيٍّ قٰتَلَ ۙ مَعَهٗ رِبِّيُّوْنَ كَثِيْرٌ ۚ فَمَا وَهَنُوْا لِمَآ اَصَابَهُمْ فِىْ سَبِيْلِ اللّٰهِ وَمَا ضَعُفُوْا وَمَا اسْتَكَانُوْا ؕ وَاللّٰهُ يُحِبُّ الصّٰبِرِيْنَ ﴿۱۴۶﴾

147. Na Manabii wangapi waliopigana, pamoja nao watakatifu wengi. Nao hawakulegea kwa yale yaliyowasibu katika njia ya Allah, wala hawakudhoofika, wala hawakujidhalilisha (mbele ya maadui). Na Allah Huwapenda wafanyao subira.

وَمَا كَانَ قَوْلَهُمْ اِلَّآ اَنْ قَالُوْا رَبَّنَا اغْفِرْ لَنَا ذُنُوْبَنَا وَاِسْرَافَنَا فِىْٓ اَمْرِنَا وَثَبِّتْ اَقْدَامَنَا وَانْصُرْنَا عَلَى الْقَوْمِ الْكٰفِرِيْنَ ﴿۱۴۷﴾

148. Wala haikuwa kauli yao ila walisema: Mola wetu, Tughofirie madhambi yetu na kupita kwetu kiasi katika mambo yetu na Uiimarishe miguu yetu na Utusaidie juu ya watu makafiri.

فَاٰتٰىهُمُ اللّٰهُ ثَوَابَ الدُّنْيَا وَحُسْنَ ثَوَابِ الْاٰخِرَةِ ؕ وَاللّٰهُ يُحِبُّ الْمُحْسِنِيْنَ ﴿۱۴۸﴾ ع

149. Hivyo Allah Aliwapa malipo ya dunia na malipo bora ya Akhera; na Allah Anawapenda wafanyao mema.

FUNGU 16

يٰٓاَيُّهَا الَّذِيْنَ اٰمَنُوْٓا اِنْ تُطِيْعُوا الَّذِيْنَ كَفَرُوْا يَرُدُّوْكُمْ عَلٰٓى اَعْقَابِكُمْ فَتَنْقَلِبُوْا خٰسِرِيْنَ ﴿۱۴۹﴾

150. Enyi mlioamini, ikiwa mtawatii waliokufuru watakurudisheni kwa visigino vyenu; hivyo mtarudi wenye hasara.

بَلِ اللّٰهُ مَوْلٰىكُمْ ۚ وَهُوَ خَيْرُ النّٰصِرِيْنَ ﴿۱۵۰﴾

151. Bali Allah ndiye Mola wenu, naye ndiye Mbora wa wasaidizi.

سَنُلْقِىْ فِىْ قُلُوْبِ الَّذِيْنَ كَفَرُوا الرُّعْبَ بِمَآ اَشْرَكُوْا بِاللّٰهِ مَا لَمْ يُنَزِّلْ بِهٖ

152. Hivi karibuni tutatia heba ndani ya mioyo ya wale waliokufuru kwa sababu ya kumshirikisha Allah

Aya 148. *Tughofirie madhambi yetu.* Kwa maana ya neno *kughofiri dhambi,* tazama sura 48:3; 11:48; na 38:24.

سُلْطٰنًا ۚ وَمَاْوٰىهُمُ النَّارُ ؕ وَبِئْسَ مَثْوَى الظّٰلِمِيْنَ ﴿۱۵۱﴾

na ambacho Hakukiteremshia dalili, na makao yao ni Motoni; na ni mabaya maskani ya wadhalimu.

وَلَقَدْ صَدَقَكُمُ اللّٰهُ وَعْدَهٗۤ اِذْ تَحُسُّوْنَهُمْ بِاِذْنِهٖ ۚ حَتّٰۤى اِذَا فَشِلْتُمْ وَتَنَازَعْتُمْ فِى الْاَمْرِ وَعَصَيْتُمْ مِّنْۢ بَعْدِ مَاۤ اَرٰىكُمْ مَّا تُحِبُّوْنَ ؕ مِنْكُمْ مَّنْ يُّرِيْدُ الدُّنْيَا وَمِنْكُمْ مَّنْ يُّرِيْدُ الْاٰخِرَةَ ۚ ثُمَّ صَرَفَكُمْ عَنْهُمْ لِيَبْتَلِيَكُمْ ۚ وَلَقَدْ عَفَا عَنْكُمْ ؕ وَاللّٰهُ ذُوْ فَضْلٍ عَلَى الْمُؤْمِنِيْنَ ﴿۱۵۲﴾

153. Na bila shaka Allah Amewasadikishieni miadi Yake mlipowaua kwa idhini Yake, mpaka mlipoonyesha woga na mkaanza kubishana ninyi kwa ninyi kuhusiana na amri yenyewe na mkaasi hata baada ya yeye kuwaonyesheni mliyoyapenda. Miongoni mwenu walikuwapo wale ambao waliitamani dunia, na miongoni mwenu walikuwako wale walioitamani Akhera. Kisha akawageuzieni mbali nao ili kuwajaribuni - naye kwa hakika Amewasameheni; na Allah ni Mwenye kuwafadhili waaminio.

اِذْ تُصْعِدُوْنَ وَلَا تَلْوٗنَ عَلٰۤى اَحَدٍ وَّالرَّسُوْلُ يَدْعُوْكُمْ فِىْۤ اُخْرٰىكُمْ فَاَثَابَكُمْ غَمًّا ۢ بِغَمٍّ لِّكَيْلَا تَحْزَنُوْا

154. (Kumbukeni) mlipokuwa mkikimbia mbio wala hamkugeuka kumsikiliza ye yote hali Mtume alikuwa akiwaiteni kutoka katika kikosi chenu kingine, Kisha Akawapeni huzuni juu ya huzuni ili msisikitikie yale

---

Aya 153. *Amewasadikishieni miadi Yake.* Yaani miadi ambayo Allah amewaahidi Waislamu mara kwa mara kuwa ushindi wote utakuwa wao.

Mlipolegea. Waliolegea ni wale Waislamu wenye mishale waliowekwa na Mtume *s.a.w.* nyuma ya jeshi la Waislamu, ili kumzuia adui asiwazunguke na kuwatokea kwa nyuma. Ingawa waliambiwa wasiondoke kilimani walipowekwa lakini tamaa ya kuteka mali za maadui waliokuwa wanaanza kushindwa na kukimbia, ikalegeza utii wao wakajitoma katika mkumbo wa kukusanya mateka. Nyuma adui akawazunguka, wasiwe tena na nafasi ya kumzuia, na mambo yakapinduka, Waislamu wakawa ndiyo wenye kushindwa.

Mkaasi. Yaani hawakumsikiliza mkubwa wao Abdullah bin Jubair ambaye kwa kufuata maagizo ya Mtume s.a.w. aliwakataza wasiondoke hata kama waone wanashinda. Wao walisambaa kufuatia mateka, na hivyo ikawa kushindwa.. Kwa hakika kutii kabisa maagizo ya mkuu au ya kiongozi, ni jambo la lazima kabisa kama watu wanataka mafanikio.

Aya 154. *Huzuni juu ya huzuni.* Mara nyingine tishio la hasara kubwa huzima maumivu ya hasara ndogo ndogo zilizopatikana kabla. Hali ya namna hiyo ilijitokeza wakati wa vita vya

عَلٰى مَا فَاتَكُمْ وَلَا مَآ اَصَابَكُمْ ؕ وَاللّٰهُ
خَبِيْرٌۢ بِمَا تَعْمَلُوْنَ ﴿١٥٣﴾

yaliyowapoteeni wala (yale) yaliyowasibuni. Na Allah Ana habari za mnayoyatenda.

ثُمَّ اَنْزَلَ عَلَيْكُمْ مِّنْۢ بَعْدِ الْغَمِّ اَمَنَةً
نُّعَاسًا يَّغْشٰى طَآئِفَةً مِّنْكُمْ ۙ
وَطَآئِفَةٌ قَدْ اَهَمَّتْهُمْ اَنْفُسُهُمْ
يَظُنُّوْنَ بِاللّٰهِ غَيْرَ الْحَقِّ ظَنَّ الْجَاهِلِيَّةِ ؕ
يَقُوْلُوْنَ هَلْ لَّنَا مِنَ الْاَمْرِ مِنْ شَيْءٍ ؕ
قُلْ اِنَّ الْاَمْرَ كُلَّهٗ لِلّٰهِ ؕ يُخْفُوْنَ فِيْٓ
اَنْفُسِهِمْ مَّا لَا يُبْدُوْنَ لَكَ ؕ يَقُوْلُوْنَ لَوْ
كَانَ لَنَا مِنَ الْاَمْرِ شَيْءٌ مَّا قُتِلْنَا هٰهُنَا ؕ
قُلْ لَّوْ كُنْتُمْ فِيْ بُيُوْتِكُمْ لَبَرَزَ الَّذِيْنَ
كُتِبَ عَلَيْهِمُ الْقَتْلُ اِلٰى مَضَاجِعِهِمْ ۚ
وَلِيَبْتَلِيَ اللّٰهُ مَا فِيْ صُدُوْرِكُمْ
وَلِيُمَحِّصَ مَا فِيْ قُلُوْبِكُمْ ؕ وَاللّٰهُ عَلِيْمٌۢ
بِذَاتِ الصُّدُوْرِ ﴿١٥٤﴾

155. Kisha baada ya huzuni Aliwateremshieni usingizi kuwapeni utulivu ambao ulilifunika kundi moja kati yenu, na kulikuwa na kundi moja waliozihofia nafsi zao, wakamdhania Allah dhana ya ujinga bila haki; wakasema: Je, tuna sauti yoyote katika uamuzi wa mambo muhimu? Sema: Hakika uamuzi wote ni wa Allah; wanaficha ndani ya nafsi zao wasiyokudhihirishia. Wanasema: Tungekuwa na sauti yoyote katika uamuzi wa jambo hili tusingeuawa hapa. Sema: Hata kama mngalikuwa majumbani mwenu bila shaka wangalitoka wale walioandikiwa mapigano kwenda mahali pa kuangukia kwao, na ili Allah Ayajaribu yaliyomo vifuani mwenu, na kuyasafisha yaliyomo mioyoni mwenu. Na Allah Anayajua yaliyomo vifuani.

اِنَّ الَّذِيْنَ تَوَلَّوْا مِنْكُمْ يَوْمَ الْتَقَى
الْجَمْعٰنِ ۙ اِنَّمَا اسْتَزَلَّهُمُ الشَّيْطٰنُ
بِبَعْضِ مَا كَسَبُوْا ۚ وَلَقَدْ عَفَا اللّٰهُ
عَنْهُمْ ؕ اِنَّ اللّٰهَ غَفُوْرٌ حَلِيْمٌ ﴿١٥٥﴾ ع ١٦ ٧

156. Hakika wale waliorudi nyuma miongoni mwenu siku ambayo majeshi mawili yalikutana, kwa yakini Shetani ndiye aliyewatelezesha kwa sababu ya baadhi ya waliyoyachuma, na bila shaka Allah Ameshawasamehe. Hakika Allah ni Msamehevu, Mpole sana.

Uhud ambapo uvumi wa kifo cha Mtukufu Mtume s.a.w. ukaondoa moja kwa moja fikira za mateso na hasara binafsi ambazo wapiganaji wa Kiislamu walizipata. Kisha habari za kuepukana kwake na kifo kukazigeuza hisia za hasara kuwa hisia za ridhaa kubwa na shukurani.

Aya 156. *Shetani ndiye aliyewatelezesha.* Yaani wale wapiga mishale hamsini waliowekwa kilimani wanaotajwa katika Aya 122 na 153 za sura hii.

FUNGU 17

يٰٓاَيُّهَا الَّذِيْنَ اٰمَنُوْا لَا تَكُوْنُوْا كَالَّذِيْنَ كَفَرُوْا وَقَالُوْا لِاِخْوَانِهِمْ اِذَا ضَرَبُوْا فِي الْاَرْضِ اَوْ كَانُوْا غُزًّى لَّوْ كَانُوْا عِنْدَنَا مَا مَاتُوْا وَمَا قُتِلُوْا ۚ لِيَجْعَلَ اللّٰهُ ذٰلِكَ حَسْرَةً فِيْ قُلُوْبِهِمْ ۭ وَاللّٰهُ يُحْيٖ وَيُمِيْتُ ۭ وَاللّٰهُ بِمَا تَعْمَلُوْنَ بَصِيْرٌ ﴿١٥٦﴾

157. Enyi mlioamini, msiwe kama wale waliokufuru na wakasema juu ya ndugu zao, waliposafiri katika nchi, au walipotoka ili kupigana, Wangalikuwa pamoja nasi wasingalikufa (namna hii) wala wasingeuawa; ili Allah Ayafanye hayo kuwa majuto katika nyoyo zao. Na Allah Anahuisha na kufisha, na Allah Anaona mnayoyatenda.

وَلَىِٕنْ قُتِلْتُمْ فِيْ سَبِيْلِ اللّٰهِ اَوْ مُتُّمْ لَمَغْفِرَةٌ مِّنَ اللّٰهِ وَرَحْمَةٌ خَيْرٌ مِّمَّا يَجْمَعُوْنَ ﴿١٥٧﴾

158. Na kama mkiuawa katika njia ya Allah au mkifa, basi msamaha na rehema kutoka kwa Allah ni bora kuliko vile wanavyokusanya.

وَلَىِٕنْ مُّتُّمْ اَوْ قُتِلْتُمْ لَاِلَى اللّٰهِ تُحْشَرُوْنَ ﴿١٥٨﴾

159. Na kama mkifa au mkiuawa, kwa yakini nyote mtakusanywa kwa Allah.

فَبِمَا رَحْمَةٍ مِّنَ اللّٰهِ لِنْتَ لَهُمْ ۚ وَلَوْ كُنْتَ فَظًّا غَلِيْظَ الْقَلْبِ لَانْفَضُّوْا مِنْ حَوْلِكَ ۠ فَاعْفُ عَنْهُمْ وَاسْتَغْفِرْ لَهُمْ وَشَاوِرْهُمْ فِي الْاَمْرِ ۚ فَاِذَا عَزَمْتَ فَتَوَكَّلْ عَلَى اللّٰهِ ۭ اِنَّ اللّٰهَ يُحِبُّ الْمُتَوَكِّلِيْنَ ﴿١٥٩﴾

160. Basi kwa sababu ya rehema itokayo kwa Allah umekuwa laini kwao; na kama ungekuwa mkali na mwenye moyo mgumu, bila shaka wangalikukimbia. Basi uwasamehe na uwaombee msamaha na ushauriane nao katika mambo (yaliyo muhimu); na ufungapo nia, basi umtegemee Allah; hakika Allah Anawapenda wamtegemeao.

اِنْ يَّنْصُرْكُمُ اللّٰهُ فَلَا غَالِبَ لَكُمْ ۚ وَاِنْ يَّخْذُلْكُمْ فَمَنْ ذَا الَّذِيْ يَنْصُرُكُمْ مِّنْۢ بَعْدِهٖ ۭ وَعَلَى اللّٰهِ فَلْيَتَوَكَّلِ الْمُؤْمِنُوْنَ ﴿١٦٠﴾

161. Ikiwa Allah Anawasaidieni, basi hakuna atakayeweza kuwashindeni; na kama Akiwaacheni, ni nani tena atakayewasaidieni baada Yake? Na wenye kuamini basi wamtegemee Allah.

Aya 160. *Umekuwa laini kwao.* Aya hii inaonyesha ilivyokuwa nzuri tabia ya Mtume *s.a.w.* Alikuwa mwenye huruma ajabu, na mwema, si kwa masahaba zake na wafuasi wake tu, bali kwa maadui zake pia ambao kila mara walitafuta kumdhuru. Hii ni moja katika siri za mafanikio ya Mtume s.a.w. Watu walimwona ni mwema na laini, wakamfuata na kumpenda na kumtii.

وَمَا كَانَ لِنَبِيٍّ اَنْ يَّغُلَّ ؕ وَمَنْ يَّغْلُلْ يَاْتِ
بِمَا غَلَّ يَوْمَ الْقِيٰمَةِ ۚ ثُمَّ تُوَفّٰى كُلُّ نَفْسٍ
مَّا كَسَبَتْ وَهُمْ لَا يُظْلَمُوْنَ ﴿۱۶۱﴾

162. Na haiwezekani kwa Nabii yeyote kufanya hiyana; na atakayefanya hiyana, atayaleta, siku ya Kiyama (matokeo mabaya ya) aliyoyahini; kisha kila nafsi itapewa sawasawa iliyoyachuma, nao hawatadhulumiwa.

اَفَمَنِ اتَّبَعَ رِضْوَانَ اللّٰهِ كَمَنْۢ بَآءَ
بِسَخَطٍ مِّنَ اللّٰهِ وَ مَاْوٰىهُ جَهَنَّمُ ؕ
وَ بِئْسَ الْمَصِيْرُ ﴿۱۶۲﴾

163. Je, aliyefuata radhi ya Allah ni kama yule aliyerudi na ghadhabu ya Allah na makao yake ni Jahanamu? Napo ni mahala pabaya pa kurejea.

هُمْ دَرَجٰتٌ عِنْدَ اللّٰهِ ؕ وَاللّٰهُ بَصِيْرٌۢ بِمَا
يَعْمَلُوْنَ ﴿۱۶۳﴾

164. Hao ni (watu) wenye vyeo mbali mbali mbele ya Allah; na Allah Huona wanayoyatenda.

لَقَدْ مَنَّ اللّٰهُ عَلَى الْمُؤْمِنِيْنَ اِذْ بَعَثَ
فِيْهِمْ رَسُوْلًا مِّنْ اَنْفُسِهِمْ يَتْلُوْا عَلَيْهِمْ
اٰيٰتِهٖ وَ يُزَكِّيْهِمْ وَ يُعَلِّمُهُمُ الْكِتٰبَ
وَالْحِكْمَةَ ۚ وَ اِنْ كَانُوْا مِنْ قَبْلُ
لَفِيْ ضَلٰلٍ مُّبِيْنٍ ﴿۱۶۴﴾

165. Hakika Allah Amefanya hisani juu ya waaminio Alipoinua Mtume kati yao kutoka miongoni mwao anayewasomea Aya Zake, na anawatakasa na kuwafundisha Kitabu na hekima; na ingawa zamani walikuwa katika upotevu dhahiri.

اَوَ لَمَّاۤ اَصَابَتْكُمْ مُّصِيْبَةٌ قَدْ اَصَبْتُمْ
مِّثْلَيْهَا ۙ قُلْتُمْ اَنّٰى هٰذَا ؕ قُلْ هُوَ مِنْ عِنْدِ
اَنْفُسِكُمْ ؕ اِنَّ اللّٰهَ عَلٰى كُلِّ شَيْءٍ قَدِيْرٌ ﴿۱۶۵﴾

166. Ala! Ninyi uwafikiapo msiba - nanyi mmekwisha watia mara mbili ya huo - mnasema: Umetokea wapi huu? Sema: Huo umetoka kwenu wenyewe. Hakika Allah ni Mwenye uwezo juu ya kila kitu.

وَمَاۤ اَصَابَكُمْ يَوْمَ الْتَقَى الْجَمْعٰنِ
فَبِاِذْنِ اللّٰهِ وَ لِيَعْلَمَ الْمُؤْمِنِيْنَ ﴿۱۶۶﴾

167. Na msiba ule uliowafikieni siku ya mkutano wa majeshi mawili ulikuwa kwa idhini ya Allah; ili Awapambanue waaminio;

وَ لِيَعْلَمَ الَّذِيْنَ نَافَقُوْا ۖۚ وَ قِيْلَ لَهُمْ تَعَالَوْا
قَاتِلُوْا فِيْ سَبِيْلِ اللّٰهِ اَوِ ادْفَعُوْا ؕ قَالُوْا لَوْ
نَعْلَمُ قِتَالًا لَّا اتَّبَعْنٰكُمْ ؕ هُمْ لِلْكُفْرِ
يَوْمَئِذٍ اَقْرَبُ مِنْهُمْ لِلْاِيْمَانِ ۚ

168. Na kuwapambanua wale waliofanya unafiki. Nao waliambiwa: Njooni mpigane katika njia ya Allah au kuzuia (maadui). Wakasema: Tungalijua kupigana bila shaka tungewafuateni. Wao siku ile walikuwa karibu zaidi na kufuru kuliko imani.

Aya 167. *Siku ya mkutano wa majeshi mawili*, yaani siku ya vita vya Uhud.

يَقُوْلُوْنَ بِاَفْوَاهِهِمْ مَّا لَيْسَ فِيْ
قُلُوْبِهِمْ ؕ وَاللّٰهُ اَعْلَمُ بِمَا يَكْتُمُوْنَ ﴿۱۶۸﴾

Wanasema kwa midomo yao yasiyokuwamo mioyoni mwao; na Allah Anayajua sana wanayoyaficha.

اَلَّذِيْنَ قَالُوْا لِاِخْوَانِهِمْ وَقَعَدُوْا لَوْ
اَطَاعُوْنَا مَا قُتِلُوْا ؕ قُلْ فَادْرَءُوْا عَنْ
اَنْفُسِكُمُ الْمَوْتَ اِنْ كُنْتُمْ صٰدِقِيْنَ ﴿۱۶۹﴾

169. Wale waliosema juu ya ndugu zao, na wao wenyewe wakakaa: wangalitutii wasingeuawa. Sema: Jiondoleeni mauti ikiwa mnasema kweli.

وَلَا تَحْسَبَنَّ الَّذِيْنَ قُتِلُوْا فِيْ سَبِيْلِ اللّٰهِ
اَمْوَاتًا ؕ بَلْ اَحْيَآءٌ عِنْدَ رَبِّهِمْ يُرْزَقُوْنَ ﴿۱۷۰﴾

170. Wala usiwadhani wale waliouawa katika njia ya Allah ni wafu. Bali wako hai, wakiruzukiwa kwa Mola wao.

فَرِحِيْنَ بِمَآ اٰتٰهُمُ اللّٰهُ مِنْ فَضْلِهٖ ۙ
وَيَسْتَبْشِرُوْنَ بِالَّذِيْنَ لَمْ يَلْحَقُوْا بِهِمْ
مِّنْ خَلْفِهِمْ ۙ اَلَّا خَوْفٌ عَلَيْهِمْ وَلَا هُمْ
يَحْزَنُوْنَ ﴿۱۷۱﴾

171. Wakifurahia Aliyowapa Allah kwa fadhili Zake; na wanawashangilia wale ambao hawajajiunga nao walio nyuma yao, ya kwamba haitakuwa hofu juu yao wala hawatahuzunika.

يَسْتَبْشِرُوْنَ بِنِعْمَةٍ مِّنَ اللّٰهِ وَفَضْلٍ ۙ
وَّاَنَّ اللّٰهَ لَا يُضِيْعُ اَجْرَ الْمُؤْمِنِيْنَ ﴿۱۷۲﴾ ع ۱۷

172. Wanapata habari za kufurahisha za neema na fadhili za Allah, na ya kwamba Allah Hapotezi ujira wa waaminio.

FUNGU 18

اَلَّذِيْنَ اسْتَجَابُوْا لِلّٰهِ وَالرَّسُوْلِ مِنْۢ بَعْدِ
مَآ اَصَابَهُمُ الْقَرْحُ ۛؕ لِلَّذِيْنَ اَحْسَنُوْا
مِنْهُمْ وَاتَّقَوْا اَجْرٌ عَظِيْمٌ ﴿۱۷۳﴾

173. Wale waliomwitikia Allah na Mtume baada ya majeraha kuwapata kwa wale waliofanya wema miongoni mwao na kumcha Mungu utakuwa ujira mkubwa.

اَلَّذِيْنَ قَالَ لَهُمُ النَّاسُ اِنَّ النَّاسَ قَدْ
جَمَعُوْا لَكُمْ فَاخْشَوْهُمْ فَزَادَهُمْ
اِيْمَانًا ۖ وَّقَالُوْا حَسْبُنَا اللّٰهُ وَنِعْمَ الْوَكِيْلُ ﴿۱۷۴﴾

174. Wale ambao watu waliwaambia: Bila shaka watu wamekwisha wakusanyikieni, kwa hiyo waogopeni; lakini (jambo hili) likawazidisha katika imani, na wakasema: Allah Ametutosha, naye ni Mlinzi Mwema.

فَانْقَلَبُوْا بِنِعْمَةٍ مِّنَ اللّٰهِ وَفَضْلٍ لَّمْ
يَمْسَسْهُمْ سُوْٓءٌ ۙ وَّاتَّبَعُوْا رِضْوَانَ اللّٰهِ ؕ
وَاللّٰهُ ذُوْ فَضْلٍ عَظِيْمٍ ﴿۱۷۵﴾

175. Basi wakarudi na neema za Allah na fadhili (Zake); hakuna hata shida iliyowagusa na wakafuata radhi ya Allah; Na Allah ni Mwenye fadhili kuu.

اِنَّمَا ذٰلِكُمُ الشَّيْطٰنُ يُخَوِّفُ اَوْلِيَآءَهٗ ۪
فَلَا تَخَافُوْهُمْ وَخَافُوْنِ اِنْ كُنْتُمْ
مُّؤْمِنِيْنَ ﴿۱۷۵﴾

176. Hakika ni Shetani ndiye huwa anawaogopesha marafiki zake, basi msiwaogope bali Niogopeni Mimi mkiwa waaminio.

وَلَا يَحْزُنْكَ الَّذِيْنَ يُسَارِعُوْنَ فِي
الْكُفْرِ ۚ اِنَّهُمْ لَنْ يَّضُرُّوا اللّٰهَ شَيْـًٔا ؕ
يُرِيْدُ اللّٰهُ اَلَّا يَجْعَلَ لَهُمْ حَظًّا فِي
الْاٰخِرَةِ ۚ وَلَهُمْ عَذَابٌ عَظِيْمٌ ﴿۱۷۶﴾

177. Wala wasikuhuzunishe wale wanaozidi katika ukafiri; hakika hao hawatamdhuru Allah cho chote. Allah Anataka Asiwawekee sehemu yo yote katika Akhera; na itakuwa kwao adhabu kubwa.

اِنَّ الَّذِيْنَ اشْتَرَوُا الْكُفْرَ بِالْاِيْمَانِ لَنْ
يَّضُرُّوا اللّٰهَ شَيْـًٔا ۚ وَلَهُمْ عَذَابٌ اَلِيْمٌ ﴿۱۷۷﴾

178. Hakika wale walionunua kufuru kwa imani, hawataweza kabisa kumdhuru Allah cho chote; na itakuwa kwao adhabu iumizayo.

وَلَا يَحْسَبَنَّ الَّذِيْنَ كَفَرُوْٓا اَنَّمَا نُمْلِيْ
لَهُمْ خَيْرٌ لِّاَنْفُسِهِمْ ؕ اِنَّمَا نُمْلِيْ لَهُمْ
لِيَزْدَادُوْٓا اِثْمًا ۚ وَلَهُمْ عَذَابٌ مُّهِيْنٌ ﴿۱۷۸﴾

179. Wala wasidhani wale wanaokufuru kwamba muda Tunaowapa ni bora kwao. Hakika Tunawapa muda ili wazidi katika madhambi; na itakuwa kwao adhabu ifedheheshayo.

مَا كَانَ اللّٰهُ لِيَذَرَ الْمُؤْمِنِيْنَ عَلٰى مَآ
اَنْتُمْ عَلَيْهِ حَتّٰى يَمِيْزَ الْخَبِيْثَ مِنَ
الطَّيِّبِ ؕ وَمَا كَانَ اللّٰهُ لِيُطْلِعَكُمْ عَلَى
الْغَيْبِ وَلٰكِنَّ اللّٰهَ يَجْتَبِيْ مِنْ رُّسُلِهٖ مَنْ

180. Haimpasi Allah kuwaacha waaminio katika hali mliyo nayo mpaka Apambanue mbaya katika mwema; wala haimpasi Allah kuwajulisheni mambo ya ghaibu, bali Allah Huchagua katika Mitume Wake Amtakaye. Basi

Aya **179.** *Wanazidi katika madhambi;* mradi wa hapa sio kuwa makusudi ya wao kupewa muda ni kwamba wazidi katika madhambi, bali ni kwamba wanapewa muda na matokeo yake yanakuwa wanazidi katika dhambi. Kama wasemavyo Waarabu. "Zaa watoto wapate kufa," siyo maana yake makusudi ya kuzaa ni kufa bali matokeo yanakuwa hivyo.

يَّشَآءُ ۚ فَاٰمِنُوْا بِاللّٰهِ وَرُسُلِهٖ ۚ وَاِنْ
تُؤْمِنُوْا وَتَتَّقُوْا فَلَكُمْ اَجْرٌ عَظِيْمٌ ﴿١٧٩﴾
وَلَا يَحْسَبَنَّ الَّذِيْنَ يَبْخَلُوْنَ بِمَآ اٰتٰىهُمُ
اللّٰهُ مِنْ فَضْلِهٖ هُوَ خَيْرًا لَّهُمْ ۭ بَلْ هُوَ شَرٌّ
لَّهُمْ ۭ سَيُطَوَّقُوْنَ مَا بَخِلُوْا بِهٖ يَوْمَ
الْقِيٰمَةِ ۭ وَلِلّٰهِ مِيْرَاثُ السَّمٰوٰتِ
وَالْاَرْضِ ۭ وَاللّٰهُ بِمَا تَعْمَلُوْنَ خَبِيْرٌ ﴿١٨٠﴾ ع

Mwaminini Allah na Mitume Wake. Na kama mtaamini na mtaogopa, basi utakuwa kwenu ujira mkubwa.

181. Wasidhani katu wale wafanyao ubakhili katika yale Aliyowapa Allah katika fadhili Zake kuwa ni bora kwao, la, ni vibaya kwao; watafungwa kongwa za yale waliyoyafanyia ubahili siku ya Kiyama; na urithi wa mbingu na ardhi ni wa Allah; na Allah daima Anazo habari za mnayoyafanya.

FUNGU 19

لَقَدْ سَمِعَ اللّٰهُ قَوْلَ الَّذِيْنَ قَالُوْٓا اِنَّ اللّٰهَ
فَقِيْرٌ وَّنَحْنُ اَغْنِيَاۗءُ ۘ سَنَكْتُبُ مَا قَالُوْا ۚ
وَقَتْلَهُمُ الْاَنْۢبِيَاۗءَ بِغَيْرِ حَقٍّ ۙ وَّنَقُوْلُ
ذُوْقُوْا عَذَابَ الْحَرِيْقِ ﴿١٨١﴾
ذٰلِكَ بِمَا قَدَّمَتْ اَيْدِيْكُمْ وَاَنَّ اللّٰهَ لَيْسَ
بِظَلَّامٍ لِّلْعَبِيْدِ ﴿١٨٢﴾
اَلَّذِيْنَ قَالُوْٓا اِنَّ اللّٰهَ عَهِدَ اِلَيْنَآ اَلَّا
نُؤْمِنَ لِرَسُوْلٍ حَتّٰى يَاْتِيَنَا بِقُرْبَانٍ تَاْكُلُهُ
النَّارُ ۭ قُلْ قَدْ جَاۗءَكُمْ رُسُلٌ مِّنْ
قَبْلِيْ بِالْبَيِّنٰتِ وَبِالَّذِيْ قُلْتُمْ فَلِمَ
قَتَلْتُمُوْهُمْ اِنْ كُنْتُمْ صٰدِقِيْنَ ﴿١٨٣﴾

182. Kwa yakini Allah Amekwisha sikia kauli ya wale waliosema: Hakika Allah ni fukara na sisi ni matajiri. Hakika Tutayaandika waliyoyasema, na pia kuwapinga kwao mno Manabii bila ya haki, na Tutawaambia onjeni adhabu ya kuungua.

183. Haya ni kwa sababu ya yale iliyoyatanguliza mikono yenu, ilhali Allah si Mwenye kuwadhulumu watumishi hata kidogo.

184. (Ama) wale waliosema: Hakika Allah Ametuahidi ya kwamba tusimwamini kabisa Mtume ye yote mpaka atuletee dhabihu inayoliwa na moto. Sema: Bila shaka wameshafika kwenu Mitume kabla yangu kwa Ishara zilizo wazi na kwa yale mliyosema. Basi kwa nini mliwapinga kama mu wakweli?

Aya 182. *Mungu ni maskini na sisi ni matajiri*. Mayahudi ndiyo waliosema maneno haya.

فَاِنْ كَذَّبُوْكَ فَقَدْ كُذِّبَ رُسُلٌ
مِّنْ قَبْلِكَ جَآءُوْ بِالْبَيِّنٰتِ وَ الزُّبُرِ
وَالْكِتٰبِ الْمُنِيْرِ ﴿۱۸۵﴾

185. Na kama wakikukadhibisha, basi wamekwisha kadhibishwa Mitume kabla yako waliofika na Ishara waziwazi na Vitabu vyenye hekima, na Kitabu chenye nuru.

كُلُّ نَفْسٍ ذَآئِقَةُ الْمَوْتِ ؕ وَ اِنَّمَا تُوَفَّوْنَ
اُجُوْرَكُمْ يَوْمَ الْقِيٰمَةِ ؕ فَمَنْ زُحْزِحَ
عَنِ النَّارِ وَ اُدْخِلَ الْجَنَّةَ فَقَدْ فَازَ ؕ وَمَا
الْحَيٰوةُ الدُّنْيَآ اِلَّا مَتَاعُ الْغُرُوْرِ ﴿۱۸۶﴾

186. Kila nafsi itaonja mauti, na bila shaka mtapewa ujira wenu sawasawa siku ya Kiyama. Na aliyewekwa mbali na Moto na kuingizwa Peponi, basi amefaulu; na maisha ya dunia hii si kitu ila ni starehe idanganyayo.

لَتُبْلَوُنَّ فِيْٓ اَمْوَالِكُمْ وَ اَنْفُسِكُمْ ۫
وَلَتَسْمَعُنَّ مِنَ الَّذِيْنَ اُوْتُوا الْكِتٰبَ مِنْ
قَبْلِكُمْ وَ مِنَ الَّذِيْنَ اَشْرَكُوْٓا اَذًى كَثِيْرًا ؕ
وَ اِنْ تَصْبِرُوْا وَتَتَّقُوْا فَاِنَّ ذٰلِكَ مِنْ
عَزْمِ الْاُمُوْرِ ﴿۱۸۷﴾

187. Kwa yakini mtajaribiwa katika mali zenu na nafsi zenu na hakika mtasikia kwa wale waliopewa Kitabu kabla yenu, na kwa wale walioshirikisha, udhia mwingi. Na kama mkisubiri na kujilinda, basi kwa hakika hilo ni katika mambo makubwa.

وَ اِذْ اَخَذَ اللّٰهُ مِيْثَاقَ الَّذِيْنَ اُوْتُوا الْكِتٰبَ
لَتُبَيِّنُنَّهٗ لِلنَّاسِ وَلَا تَكْتُمُوْنَهٗ ۫
فَنَبَذُوْهُ وَرَآءَ ظُهُوْرِهِمْ وَاشْتَرَوْا بِهٖ
ثَمَنًا قَلِيْلًا ؕ فَبِئْسَ مَا يَشْتَرُوْنَ ﴿۱۸۸﴾

188. Na (kumbuka) Allah Alipofunga ahadi na wale waliopewa Kitabu: Lazima mtakibainisha kwa watu wala hamtakificha. Lakini walikitupa nyuma ya migongo yao, na wakakiuza kwa thamani ndogo. Basi ni mabaya wanayoyanunua.

لَا تَحْسَبَنَّ الَّذِيْنَ يَفْرَحُوْنَ بِمَآ اَتَوْا
وَّ يُحِبُّوْنَ اَنْ يُّحْمَدُوْا بِمَا لَمْ يَفْعَلُوْا
فَلَا تَحْسَبَنَّهُمْ بِمَفَازَةٍ مِّنَ الْعَذَابِ ۚ
وَلَهُمْ عَذَابٌ اَلِيْمٌ ﴿۱۸۹﴾

189. Usidhani wanaofurahia mambo waliyoyafanya, na wanapenda kusifiwa kwa yale wasiyoyafanya - basi usidhani kuwa ni wenye kusalimika na adhabu; bali itakuwa kwao adhabu iumizayo.

وَ لِلّٰهِ مُلْكُ السَّمٰوٰتِ وَالْاَرْضِ ؕ وَاللّٰهُ
عَلٰى كُلِّ شَيْءٍ قَدِيْرٌ ﴿۱۹۰﴾ ع ۱۹

190. Na ufalme wa mbingu na ardhi ni wa Allah; na Allah ni Mwenye uwezo juu ya kila kitu.

FUNGU 20

191. Kwa hakika katika uumbaji wa mbingu na ardhi na mfuatano wa usiku na mchana ziko Ishara kwa wenye akili;

اِنَّ فِیْ خَلْقِ السَّمٰوٰتِ وَ الْاَرْضِ وَ اخْتِلَافِ الَّیْلِ وَ النَّهَارِ لَاٰیٰتٍ لِّاُولِی الْاَلْبَابِ ﴿۱۹۱﴾

192. Ambao humkumbuka Allah wakiwa wima na wakikaa na wakilala kibavu na huutafakari uumbaji wa mbingu na ardhi: Mola wetu, Hukuviumba hivi bure; utukufu ni Wako, basi Utuepushe na adhabu ya Moto.

الَّذِیْنَ یَذْكُرُوْنَ اللّٰهَ قِیٰمًا وَّ قُعُوْدًا وَّ عَلٰی جُنُوْبِهِمْ وَ یَتَفَكَّرُوْنَ فِیْ خَلْقِ السَّمٰوٰتِ وَ الْاَرْضِ ۚ رَبَّنَا مَا خَلَقْتَ هٰذَا بَاطِلًا ۚ سُبْحٰنَكَ فَقِنَا عَذَابَ النَّارِ ﴿۱۹۲﴾

193. Mola wetu, hakika yule ambaye Umemwingiza Motoni, basi Umekwisha mfedhehesha, na hawatakuwapo wasaidizi kwa ajili ya wadhalimu.

رَبَّنَاۤ اِنَّكَ مَنْ تُدْخِلِ النَّارَ فَقَدْ اَخْزَیْتَهٗ ؕ وَ مَا لِلظّٰلِمِیْنَ مِنْ اَنْصَارٍ ﴿۱۹۲﴾

194. Mola wetu, hakika tumemsikia Mwitaji akiita kwenye imani ya kwamba Mwaminini Mola wenu. Basi tumeamini. Mola wetu, Utusamehe madhambi yetu na Utuondolee maovu yetu na Utufishe pamoja na watu wema.

رَبَّنَاۤ اِنَّنَا سَمِعْنَا مُنَادِیًا یُّنَادِیْ لِلْاِیْمَانِ اَنْ اٰمِنُوْا بِرَبِّكُمْ فَاٰمَنَّا ۟ رَبَّنَا فَاغْفِرْ لَنَا ذُنُوْبَنَا وَ كَفِّرْ عَنَّا سَیِّاٰتِنَا وَ تَوَفَّنَا مَعَ الْاَبْرَارِ ۚ ﴿۱۹۳﴾

195. Mola wetu, na Ututimizie ile ahadi uliyoilazimisha kwa Mitume Wako kwa ajili yetu, wala Usitufedheheshe siku ya Kiyama; bila shaka Wewe Huvunji miadi.

رَبَّنَا وَ اٰتِنَا مَا وَعَدْتَّنَا عَلٰی رُسُلِكَ وَ لَا تُخْزِنَا یَوْمَ الْقِیٰمَةِ ؕ اِنَّكَ لَا تُخْلِفُ الْمِیْعَادَ ﴿۱۹۴﴾

196. Ndipo Mola wao Akakubali maombi yao (kwa kusema), Hakika Mimi Sitapoteza amali ya mfanya juhudi miongoni mwenu, awe mwanamume au mwanamke, ni ninyi kwa ninyi. Basi waliohama na kufukuzwa katika majumba yao na kupewa udhia katika njia Yangu, na wakapigana na kuuawa, kwa Yakini

فَاسْتَجَابَ لَهُمْ رَبُّهُمْ اَنِّیْ لَاۤ اُضِیْعُ عَمَلَ عَامِلٍ مِّنْكُمْ مِّنْ ذَكَرٍ اَوْ اُنْثٰی ۚ بَعْضُكُمْ مِّنْۢ بَعْضٍ ۚ فَالَّذِیْنَ هَاجَرُوْا وَ اُخْرِجُوْا مِنْ دِیَارِهِمْ وَ اُوْذُوْا فِیْ سَبِیْلِیْ وَ قٰتَلُوْا وَ قُتِلُوْا لَاُكَفِّرَنَّ

Aya 196. *Akiwa mwanamume au mwanamke.* Dini ya Kiislamu ndiyo dini ya kwanza katika dunia kuhifadhi haki za wanawake, na kuwapa heshima kwa namna ambayo hawakupata

Nitawafutia makosa yao, na kwa yakini Nitawaingiza katika mabustani yanayopita mito ndani yake, ndiyo malipo kutoka kwa Allah, Na Allah kwake kuna malipo mema.

عَنْهُمْ سَيِّاٰتِهِمْ وَ لَاُدْخِلَنَّهُمْ جَنّٰتٍ تَجْرِیْ مِنْ تَحْتِهَا الْاَنْهٰرُ ثَوَابًا مِّنْ عِنْدِ اللّٰهِ ؕ وَ اللّٰهُ عِنْدَهٗ حُسْنُ الثَّوَابِ ﴿۱۹۵﴾

kuhifadhiwa au kupewa na dini nyingine yo yote kabla. Padre Dale anasema, "Lakini twaweza kusema ya kuwa katika dini ya Kikristo wanawake wana cheo cha heshima kuliko wanawake wa Kiislamu katika dini yao" (uk. 568 - 569). Maneno haya ya Padre yanaweza kumdanganya Mkristo asiye na habari ya mafundisho ya Kiislamu au anayepata habari za juu juu; au yanaweza kumdanganya Mwislamu asiye na habari za mafundisho ya Vitabu vya Wakristo juu ya wanawake. Tunashangaa kuona Padre Dale amesema tu bila kueleza hayo mafundisho yao yanayopita ya Uislamu kwa kuhusu wanawake ni yepi.

ISLAM INAWAHESHIMU WANAWAKE.

Dini ya Kiislamu inaeleza ya kuwa wanawake na wanaume wameumbwa katika nafsi moja (sura 4:2). Mtume *s.a.w.* akasema, Mtu anayewafunza binti zake adabu njema na kuwapa malezi mema, mtu huyo ataingia Peponi (Bukhari na Muslim). Mwanamke hawezi kuolewa bila hiyari yake. Anapoolewa mumewe akiwa mtu mbaya, au ameona hana haja naye, ana haki ya kuachika. Ni lazima kwa mwanamke kupata elimu kama ilivyo lazima kwa mwanamume (Muslim). Mwanamke anayo haki ya kurithi katika mali zinazoachwa na baba yake, mume wake, mtoto wake na ndugu wengine wanaokaribia (sura 4). Wanawake wanaweza kuwafunza wanaume, na Bi Aisha, mkewe Mtume *s.a.w.* alikuwa akiwafunza elimu masahaba wa Mtume s.a.w. (Tirmidhi). Mtume *s.a.w.* akasema, Pepo iko chini ya miguu ya mama (Musnad Ahmad, Nasai, Baihaki). Mtume *s.a.w.* akasema. Mbora wenu ni yule aliye mbora kwa wakeze (Tirmidhi, Ibni Maja). Mtume *s.a.w.* akasema, Mwenye kumwangalia mjane na maskini atapata thawabu ya Haji na Jihadi (Bukhari, Muslim). Bi Halima, ambaye alimnyonyesha Mtume s.a.w. siku moja alifika kwa Mtume, na Mtume alimpokea kwa heshima sana na akamtandikia shuka yake kukalia (Dawud). Binti yake alipokuwa akifika kwake, Mtume alikuwa akimsimamia. Mwanamke wa Kiislamu anaweza kumiliki mali yake mwenyewe bila mumewe au mtu mwingine kuwa na haki ya kujiingiza. Wanawake wamepewa haki zao zote na dini ya Kiislamu wala hakuna awezaye kuonyesha haki yo yote waliyonyimwa iliyo hasa ni haki yao. Naam, mume amepewa daraja juu ya mkewe katika kukata mashauri ya nyumbani, maana yeye ndiye mvumbuzi wa matumizi na shauri lake lazima liwe la mwisho. Na hii ndiyo desturi maana kila kazi na kila umoja huwa na kiongozi anayekata shauri baada ya kushauriana na wenziwe, wala daraja ya kiasi hicho haimpi mtu mwenye akili kuhesabu kuwa ni kudharauliwa.

UKRISTO NA WANAWAKE

Lakini dini ya Kikristo imewapa wanawake heshima gani? Mwanzo tu wa kuumbwa watu mwanamke anaambiwa: "Tamaa yako itakuwa ikimwelekea mumeo, naye atatawala juu yako" (Mwanzo 3:16). Tena mwanamke anaambiwa, "Wala mwanamume hakuumbwa kwa ajili ya mwanamke, bali mwanamke kwa ajili ya mwanamume" (1 Wakorintho 11:9). Mwanamke ameitwa ni kitu kilicho kichafu ambaye kitu kisafi hakiwezi kutolewa ndani yake (Ayubu 14:1-4) na 15:14); na Sulemani alimtoa mkewe binti Farao katika mji wa Daudi ili mkewe huyo asikae huko kwa kuwa mwahali mle ni mtakatifu (2 Mambo ya nyakati 8: 11). Mwanamke "ataokolewa kwa uzazi wake" (1 Timetheo 2:15). Ndiyo kusema, kama asizae, maneno hayo hayamwahidi kuokoka. "Kichwa cha mwanamke ni mwanamume" (1 Wakorintho 11:3). "Mume ni kichwa cha mke"

(Waefeso 5:23). wanawake wasijipambe "kwa kusuka nywele, wala kwa dhahabu na lulu, wala kwa nguo za thamani" (1 Timotheo 2:9). "Kujipamba kwao kusiwe kujipamba kwa nje, kusuka nywele, na kujitia dhahabu, na kuvalia mavazi" (1 Petro 3:3). Mwanamume "ni mfano wa utukufu wa Mungu, Lakini mwamamke ni utukufu wa mwanamume. Maana mwanamume hakutoka katika mwanamke, bali mwanamke katika mwanamume. Wala mwanamume hakuumbwa kwa ajili ya mwanamke, bali mwanamke kwa ajili ya mwanamume. Kwa hiyo inampasa mwanamke awe na dalili ya kumilikiwa kichwani pake" yaani kichwa chake kifunikwe (1 Wakorintho 11: 6-10). "Simpi mwanamke ruhusa kufundisha, wala kumtawala mwanamume bali kuwa katika utulivu. Kwa maana Adamu ndiye aliyeumbwa kwanza na hawa baadaye. Na Adamu hakudanganywa, bali mwanamke akidanganywa aliingia hali ya kukosa." (1 Timetheo 2:12-14). "Wanawake wanyamaze katika kanisa, maana hawana ruhusa kunena; bali watii, kama vile inenavyo torati nayo. Nao wakitaka kujifunza neno lo lote, na wawaulize waume zao wenyewe nyumbani mwao; maana ni aibu wanawake kunena katika kanisa" (1 Wakorintho 14:34-36).

Je, kuna mwanamke ye yote aliyelelewa kiungwana anayeweza kusoma mafundisho hayo ya dini ya Kikristo ya kuwadhalilisha mno bila kukunja uso?

YESU ALIWATENDEA VIPI?

Zaidi ya hayo, mwanamke mmoja Mkananaya alimfikia Yesu na kumwinamia kwa adabu "akinena, Bwana, nisaidie." Yesu "akajibu akasema. Si vema kukitwaa chakula cha watoto na kuwatupia mbwa" (Matt. 15:26). Je, kama mwanamke yule angekuwa mustahiki angeona uchungu namna gani kuitwa mbwa.

Siku moja mama wa Yesu na nduguze walitaka kuonana na Yesu, naye alikuwa katika mkutano, nao wakasimama nje. "Mtu kamwambia, tazama, mama yako na ndugu zako wamesimama nje, wanataka kusema nawe. Akajibu, akamwambia yule aliyempa khabari, Mama yangu ni nani? Na ndugu zangu ni nani? Akawanyoshea mkono wanafunzi wake, akasema, tazama Mama yangu na ndugu zangu" (Matt. 12:47-49). Je, mtu kusema maneno ya namna hii juu ya mama yake ndiyo adabu au kuwatukuza wanawake?

Siku moja katika arusi, watu walitindikiwa ulevi, na mama wa Yesu akamwambia mwanawe, Yesu, ya kwamba watu hawana ulevi. Majibu aliyotoa Yesu kumwambia mama yake yameandikwa kwa Kiingereza hivi, *"Women, what have I to do with thee?"* Yaani, "Mwanamke, mimi nina nini na nawe?" Ni wazi kwamba kumwambia mama aliyekuzaa maneno ya namna hii ni kama kudharau wanawake wote. Wakristo mpaka hivi leo bado wanaona haya kufasiri neno "Woman" "mwanamke" mahali hapo katika injili za Kiswahili. Badala ya neno mwanamke wanatumia neno "Bibi" ambalo ni lenye heshima zaidi, ingawa Yesu mwenyewe hakutumia neno hilo, na hivyo ni kama kutaka kumsahihisha, ikiwa ni yeye aliyesema vile. La, si kumsahihisha Yesu tu, bali kutupoteza na sisi tunaosoma Injili za Kiswahili tu, maana hatutajua ni kosa gani alilofanya Yesu kwa kutumia neno "mwanamke" kumwita mama yake mzazi. Hata hivyo Injili za lugha nyingine kama Kiingereza bado zina neno hilo hilo "Mwanamke". Kadhalika Injili ya Kijaluo ina neno "dhako", yaani "mwanamke". Injili ya Kiluhya pia bado ina neno hilo hilo, "Omukhasi," yaani "mwanamke." Tena Injili ya Wakatoliki iliyotangazwa mwaka 1914 inalo neno hilo hilo "mwanamke." Lakini juhudi ya kubadili neno hilo bado inaendelea kufanywa. Injili ya Wakatoliki ya mwaka 1923 imeandikwa neno "Bibi" (si "mwanamke" tena), na ya mwaka 1947 wamempandisha cheo zaidi na kuandika "Bi-mkubwa." Injili za Waprotastanti mpaka mwaka 1949 zilikuwa na neno "bibi" lakini ya mwaka uliofuata 1950 nao pia wamelipindua tena, sasa linasomeka, "mama".

HOJA YA PADRE DALE

Kurejea habari yetu, tunaweza kusema bila wasiwasi ya kuwa Padre Dale hawezi kujidai kuwa dini ya Kikristo imewapa wanawake heshima kuliko wanayopewa na dini ya Kiislamu. Kila

197. Usikudanganye hata kidogo kuja mara kwa mara katika miji, kwa wale waliokufuru.

لَا يَغُرَّنَّكَ تَقَلُّبُ الَّذِيْنَ كَفَرُوْا فِي الْبِلَادِ ﴿١٩٧﴾

198. Ni starehe ndogo. Kisha makao yao yatakuwa Jahanamu; na ni mahali pabaya palioje pa kupumzikia!

مَتَاعٌ قَلِيْلٌ ثُمَّ مَاْوٰىهُمْ جَهَنَّمُ وَبِئْسَ الْمِهَادُ ﴿١٩٨﴾

199. Lakini waliomcha Mola wao watapata Mabustani yanayopita mito chini yao; watakaa humo milele, ndiyo makaribisho toka kwa Mola wao. Na kilichoko kwa Allah ni bora kwa watu wema.

لٰكِنِ الَّذِيْنَ اتَّقَوْا رَبَّهُمْ لَهُمْ جَنّٰتٌ تَجْرِيْ مِنْ تَحْتِهَا الْاَنْهٰرُ خٰلِدِيْنَ فِيْهَا نُزُلًا مِّنْ عِنْدِ اللّٰهِ وَمَا عِنْدَ اللّٰهِ خَيْرٌ لِّلْاَبْرَارِ ﴿١٩٩﴾

200. Na kwa yakini katika watu wa Kitabu wako wanaomwamini Allah na yaliyoteremshwa kwenu na yaliyoteremshwa kwao, kwa kumnyenyekea Allah. Hawaziuzi Aya za Allah kwa thamani ndogo; hao ndio wana ujira wao kwa Mola wao. Kwa hakika Allah ni Mwepesi wa kuhesabu.

وَاِنَّ مِنْ اَهْلِ الْكِتٰبِ لَمَنْ يُّؤْمِنُ بِاللّٰهِ وَمَآ اُنْزِلَ اِلَيْكُمْ وَمَآ اُنْزِلَ اِلَيْهِمْ خٰشِعِيْنَ لِلّٰهِ لَا يَشْتَرُوْنَ بِاٰيٰتِ اللّٰهِ ثَمَنًا قَلِيْلًا اُولٰٓئِكَ لَهُمْ اَجْرُهُمْ عِنْدَ رَبِّهِمْ اِنَّ اللّٰهَ سَرِيْعُ الْحِسَابِ ﴿٢٠٠﴾

---

atakayelinganisha mafundisho ya dini hizi mbili hapa juu ataona ni dini ya Kiislamu inayostahili kusifiwa kwa kuwatukuza wanawake.

Lakini hoja aliyoona Padre dale ni kusema, "Hatuna wajakazi wala masuria katika dini yetu. Ni haramu kabisa" (uk. 569). Ndicho kijembe anachowapiga Waislamu ya kuwa dini yao ina wajakazi na masuria.

WAJAKAZI NA WATUMWA KATIKA BIBLIA

Habari za wajakazi na masuria zimeelezwa mahali pake (tazama sura 4:25, na 24:34). Na hapa tutabatilisha hoja zake kwa maneno mafupi: (1) Kama ni kweli dini yao haina wajakazi na masuria, ilikuwaje Yakobo baba wa Waisraeli wote kuwa na wajakazi? (Mwanzo 29:16-30). Ilikuwaje Daudi babu wa Yesu Kristo kuwa na masuria? (2 Samuel 12:8 na 15:16). Tena ilikuwaje Sulemani aliyejenga hekalu la Mungu kuwa na masuria mia tatu? (1 Wafalme 11:13). Je, watu wenye Vitabu vyenye habari hizi wanaweza kusema dini yao haina masuria na wajakazi? Injili nayo inasemaje juu ya jambo hili? Inasema: "enyi watumwa watiini walio bwana zenu kwa jinsi ya mwili, kwa hofu na kutetemeka, kwa unyofu wa moyo, kama kwamba ni kumtii Kristo"

201. Enyi mlioamini, subirini na subirisheni, na kuweni imara katika kuihami mipaka, na mcheni Allah ili mpate kufaulu.

يَاَيُّهَا الَّذِيْنَ اٰمَنُوا اصْبِرُوْا وَصَابِرُوْا وَ رَابِطُوْا ۟ وَ اتَّقُوا اللّٰهَ لَعَلَّكُمْ تُفْلِحُوْنَ ﴿۲۰۰﴾ ع ۲۰ ۱۱

(Waefeso 6:5). "Ninyi watumwa watiini hao ambao kwa mwili ni bwana zenu, katika mambo yote" (Wakolosai 3:22). Je, penye watumwa patakosa wajakazi na masuria?

Hivyo kujidai kuwa dini yao inaheshimu wanawake sababu haina wajakazi na masuria si maneno ya kweli hata kidogo. Maneno mengi tuliyokwisha andika yanaonyesha dini yao haiwapi wanawake heshima ya maana. Ama heshima wanayopewa leo wanawake walio nchi za Kikristo haitokani na dini, bali inatokana na maendeleo ya dunia ambayo yanaelekea kupuuza mafundisho mengi ya Kikristo. Na hata hivyo, dunia hii haijamletea mwanamke wala haitamletea heshima zaidi kuliko inayohifadhiwa na dini ya Kiislamu kwa ajili ya mwanamke.

Aya 201. *Raabituu,* "Kuweni imara", mradi wake ni: Vumilieni katika mapigano na adui zenu; au fungeni farasi wenu tayari-tayari mipakani; au endeleeni kukaa katika mipaka ya adui mkijiweka tayari; au fanyeni juhudi daima kutimiza yanayohitajiwa na dini yenu; au angakieni nyakati za sala (Lane na Akrab). Tukiunganisha maana za neno hili na maneno mengine yaliyomo katika Aya, tunapata sharti tano za mafanikio, nazo ni hizi: (1) Kufanya subira na uvumilivu kabisa; (2) Kuonyesha subira kubwa zaidi na uvumilivu mkubwa kuliko adui; (3) kufanya kwa juhudi na kwa kudumu kazi za dini na za Jumuiya; (4) kulinda barabara mipaka kwa kusudi la kuzuia mashambulio au kwa kushambulia na (5) kukaa maisha ya kitawa na kumcha Mungu. Hizi ndizo dawa za kuponya magonjwa ya Waislamu, lakini, oh, zinapuuziliwa mbali!

سُوْرَةُ النِّسَآءِ مَدَنِيَّةٌ وَّ هِيَ مَعَ الْبَسْمَلَةِ مِائَةٌ وَّ سَبْعٌ وَّ سَبْعُوْنَ اٰيَةً وَّ اَرْبَعَةٌ وَّ عِشْرُوْنَ رُكُوْعًا

4. SURA AN-NISAA

Imeteremshwa Madina

Ina mafungu 24 na Aya 177 pamoja na Bismillahi

بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ ①

1. Kwa jina la Allah, Mwingi wa rehema, Mwingi wa ukarimu.

يٰۤاَيُّهَا النَّاسُ اتَّقُوْا رَبَّكُمُ الَّذِيْ خَلَقَكُمْ مِّنْ نَّفْسٍ وَّاحِدَةٍ وَّ خَلَقَ مِنْهَا زَوْجَهَا وَ بَثَّ مِنْهُمَا رِجَالًا كَثِيْرًا وَّ نِسَآءً ۚ وَ اتَّقُوا اللّٰهَ الَّذِيْ تَسَآءَلُوْنَ بِهٖ وَ الْاَرْحَامَ ؕ اِنَّ اللّٰهَ كَانَ عَلَيْكُمْ رَقِيْبًا ②

2. Enyi watu! mcheni Mola wenu ambaye Amewaumbeni kutoka katika nafsi moja, na Ameumba kutoka katika nafsi ile nafsi yenzie, na kutoka katika nafsi hizo mbili Akaeneza wanaume wengi na wanawake; na Mcheni Allah Ambaye mnaombana kwa jina Lake na mzingatie undugu; hakika Allah ni Mlinzi juu yenu.

وَ اٰتُوا الْيَتٰمٰۤى اَمْوَالَهُمْ وَ لَا تَتَبَدَّلُوا الْخَبِيْثَ بِالطَّيِّبِ ۪ وَ لَا تَاْكُلُوْۤا اَمْوَالَهُمْ اِلٰۤى اَمْوَالِكُمْ ؕ اِنَّهٗ كَانَ حُوْبًا كَبِيْرًا ③

3. Na wapeni mayatima mali zao, wala msibadilishe mazuri kwa mabaya, wala msile mali zao pamoja na mali zenu; hakika hiyo ni dhambi kubwa.

وَ اِنْ خِفْتُمْ اَلَّا تُقْسِطُوْا فِي الْيَتٰمٰى فَانْكِحُوْا مَا طَابَ لَكُمْ مِّنَ النِّسَآءِ مَثْنٰى

4. Na kama mkiogopa kwamba hamtaweza kufanya uadilifu kuhusiana na mayatima basi waoeni wanawake

---

Bibi Aisha anaeleza ya kwamba sura hii ilifunuliwa yeye alipokwisha ingia arusi nyumbani kwa Mtume *s.a.w.* Na kwa kuwa arusi ya Bibi Aisha iliingia baada ya Hijra ni wazi ya kuwa sura hii ilishuka Madina. Kurtubi anasema ya kuwa Aya 58 ilishuka Makka wakati iliposhindwa. Lakini ni wazi ya kuwa kila Aya iliyoteremshwa baada ya Hijra ni ya Madina hata kama ishuke Makka. Neno An-Nisaa maana yake ni "Wanawake."

Aya 3. *Msibadilishe mazuri kwa mabaya,* yaani msipowapa mayatima mali zao, basi mali zenu safi zitakuwa si safi nanyi wenyewe mtapata taabu baadaye.

Msile mali zao pamoja na mali zenu. Walinzi wa mayatima wanaonywa wasichanganye mali za mayatima pamoja na zao ili wapate kuzitumia kama zao. Na kama mlinzi wa mayatima ni mtu mwenye nafasi basi asichukue malipo yo yote katika mali za mayatima. Pia tazama sura 2:216, 221.

Aya 4. *Oeni.* Ruksa ya kuoa wake wasiozidi wanne imetolewa katika Aya hii kunapotokea sababu zinazomfanya mtu ahitaji wake zaidi. Katika Aya hii sababu moja imeelezwa, ya kwamba kwa kutaka kuwatunza mayatima vizuri mtu anaweza kuhitaji wake zaidi. Sababu zingine ni kama hizi zifuatazo:-

وَثُلٰثَ وَرُبٰعَ ۚ فَاِنۡ خِفۡتُمۡ اَلَّا تَعۡدِلُوۡا
فَوَاحِدَةً اَوۡ مَا مَلَكَتۡ اَيۡمَانُكُمۡ ؕ ذٰلِكَ
اَدۡنٰۤى اَلَّا تَعُوۡلُوۡا ؕ۳

wawili au watatu au wanne muwapendao. Lakini mkiogopa kuwa hamwezi kufanya uadilifu, basi (oeni) mmoja tu, au wale ambao mikono yenu ya kuume imewamiliki; Hii ndiyo njia ya karibu zaidi kwa ajili yenu ili kuepukana na kutokufanya uadilifu.

---

(1) Mtu anao mayatima anaowatunza na kati yao mna wasichana. Yeye mwenyewe hana mke, na kwa hiyo kuna hatari ya kushawishika. Basi anaweza kuoa msichana mmoja au zaidi katika wao, na kwa njia hii aepukane na kuvunja uaminifu.

(2) Mtu ana mke lakini mkewe huyu hakai vizuri na wale mayatima. Hapo anaweza kumwoa mmoja wa mayatima wale ili nao wawe na makao ya peke yao yaliyo mazuri.

(3) Mtu amebaki na nduguze wadogo pamoja na dadaze baada ya kufariki baba yao. Na anaona ya kuwa mke aliye naye hawatazami vizuri. Hapo anaweza kuoa mwanamke mwenye umri mkubwa awezaye kukaa nao kama mama yao. Inasimuliwa ya kwamba Jabir, kijana aliyekuwa mmoja katika masahaba mashuhuri, alimwoa mwanamke mwenye umri mkubwa. Mtume *s.a.w.* alimwuliza kwa nini hakuoa kijana. Akajibu ya kuwa amefanya hivyo ili bibi huyo aweze kuwaangalia nduguze wadogo waliobaki mayatima baada ya kufariki baba yao. Mtume *s.a.w.* alipendezewa sana na tendo hili la Jabir na akamwombea dua.

(4) Kama mtu ana hofu ya kwamba kwa kuwa mayatima anaowaangalia si jamaa zake, na kwa hiyo huenda apuuze kuwatendea haki zinazostahili, basi anaweza kuunga udugu nao kwa kumwoa mmoja wao.

(5) Kama mtu anao mayatima wengi anaowalea na anaona ya kwamba mke mmoja aliye naye hatoshi kwa kuwaangalia, anaweza kuoa wake zaidi, lakini asizidi wanne.

Inasimuliwa ya kwamba, Aya hii iliposhuka, Mtume *s.a.w.* aliwaambia masahaba wake waliokuwa na zaidi ya wake wanne, waache wengine na wabaki na wanne (Tirmidhi).

Baadhi ya Wakristo wamelaumu sana ruhusa hii ya kuoa zaidi ya mke mmoja ikiwa mtu ana haja. Nasi tunapouchunguza upinzani wao hatuoni wakitoa sababu zozote zenye maana, isipokuwa kufuata tu shauku na mazoea waliyokuzwa nayo chini ya uongozi usio na busara wa makanisa na mila za makabila yao. Na linalozidi kusikitisha ni kwamba wamewaharibia hata baadhi ya watu ambao desturi hii ni yenye manufaa kwao kwa njia nyingi.

Jambo la kwanza kukumbuka ni hili ya kuwa dini ya Kiislamu siyo iliyoanzisha desturi ya kuoa wake zaidi, Ni desturi ya kale kabisa. Kabla ya Uislamu, Waarabu, kama vile watu wengine walioko hata leo, walioa wake kadiri yo yote waliyotaka. Dini ya Kiislamu inayojua kiasi, iliwaamuru wasioe zaidi ya wake wanne.

SABABU ZA KUOA WAKE WENGI

Sababu za ndoa zilizoelezwa na Qur'an ni nne: (1) Kujilinda na maradhi ya kimwili na ya kiroho na kuweka murua mwema, kwa kumfanya mtu awe na uwezo wa kutosha kujiepusha na zinaa (sura 4:25); (2) Kupata utulivu wa moyo na kuwepo mwenzi mwenye mahaba, na kuwepo stara na starehe kama zinavyositiri libasi (sura 30:22 na 2:188); (3) Kuzaa watoto na kukuza taifa la watu (sura 2:224); (4) Kupanua ujamaa na nasabu (sura 25:55).

(1) Kuna wanaume wenye matamanio makali na nguvu kubwa. Wao wasingetoshwa na mke mmoja. Islam ingezuia kuoa wake zaidi, watu wenye jinsi hii wasingefaidishwa na dini, na japo wawe na nia ya kujitakasa namna gani, lakini budi wangeshindwa na tamaa hii ambayo ina nguvu kuliko tamaa nyingine.

(2) Kama mke ni mgonjwa-mgonjwa daima, au amelemaa kabisa. au amepata wazimu, au ukoma, mume hawezi kupata utulivu. Kumfukuza mkewe si jambo la murua na ni aibu kwa vile wamekaa dahari nyingi kwa wema, na sasa ni wajibu wa mume kumwuguza mkewe. Na dini ya Kiislamu ingekataza kuoa zaidi kama ikatazavyo dini ya Kikristo basi mume huyo angekuwa amedhulumiwa bure, na mwishowe angetenda maovu kwa kushurutishwa.

(3) Kama mke ni tasa, na mtu ana haja ya watoto wa kuendeleza jina lake na ukoo wake, bila kuoa mke mwingine hawezi kamwe kupata starehe ya kufurahi na vitoto vya damu yake, na ambavyo pengine vingemfaa vitakapokua, naye kawa mzee na aliyechoka. Hivyo, Uislamu haukufanya ujinga uliofanywa na mapadre kukataza kuoa zaidi.

(4) Tena dini ya Kiislamu inaamuru kuoa wanawake wajane (sura 24:33). Na Padre Dale anasema, "Baada ya Ohod palikuwa na wajane wengi na yatima wa kike wengi" (uk. 569 wa Tafsiri yake). Sasa kama kusiwe ruksa ya kuoa wake zaidi, wajane hao wangeolewa na nani? Waachwe tu waharibike na waharibu watu? Dini ya Kikristo hapa ingefanyaje? Kwa mfano hivi leo katika nchi za Ulaya baada ya wanaume wengi kufa vitani, kumebaki mamilioni ya wanawake vijana wasio na tumaini la kupata waume. Uovu unaotapakaa huko ni wa namna ambayo ukisikia utadhani unadanganywa. Na yote hayo ni kwa sababu Ukristo umekwisha wawekea mila ya kuoa mke mmoja tu na kuwaharimishia kuoa zaidi. Baada ya mambo haya yanayoshuhudiwa, ni nani tena mwenye kuthubutu kulaumu ruhusa hii bora ya kuoa zaidi, endapo mtu ana haja na anao uwezo wa kujiweka vema yeye na wakeze?

Kwa desturi, baada ya vita, watu hupungua sana. Leo hii Ulaya haitoweza kupona katika kupungukiwa na watu ambao wangehitajiwa kuwa askari na kufanya kazi zingine za vita; na kadhalika haitapona katika uharibifu uliowaingilia sharti waachilie mbali maoni yao yenye makosa juu ya jambo hili na kuruhusu watu kuoa zaidi.

UPINZANI UNAJIBIWA

Upinzani wa mapadre juu ya jambo hili kwa hakika unachusha. Wanapenda kulaumu bila kujali ubora wa jambo lenyewe ila tu kwa kuwa wao wenyewe hawanalo jambo hili kwa ajili ya kuharibiwa na watangulizi wao. Padre Dale anasema. Wakristo hawawezi kuiamini Qur'an kwa kuwa Vitabu vyao havipatani na Qur'an (uk. 583). Je, Ukristo unapatana na mafundisho ya Agano la Kale? Mbona wanaamini Agano la Kale pia? Katika shauri la vyakula, ibada na hukumu nyingine za dini, Ukristo ni mbali na Agano la Kale, lakini juu ya kuhitilafiana hivyo, wanaamini Agano la Kale pia.

Kadhalika Padre Dale anasema. "Mkristo hapewi ruhusa katika Injili kuwa na wake wawili, sembuse wanne" (uk 569). Lakini Injili inasema, Yesu alisema, "Msidhani ya kuwa nalikuja kuitangua Torati au manabii; la, sikuja kutangua, bali kutimiliza. Kwa maana, amin, nawaambia, mpaka mbingu na nchi zitakapoondoka, yodi moja wala nukta moja ya Torati haitaondoka, hata yote yatimie. Basi mtu ye yote atakayevunja amri moja katika hizi zilizo ndogo, na kuwafundisha watu hivyo, ataitwa mdogo kabisa katika ufalme wa mbinguni; bali mtu atakayezitenda na kuzifundisha, huyo ataitwa mkubwa katika ufalme wa mbinguni (Matt. 5:17-20). Tena Yesu akasema "Waandishi na Mafarisayo wameketi katika kiti cha Musa; basi yo yote watakayowaambia myashike na kuyatenda" (Matt. 23:2).

BIBLIA INARUHUSU WAKE WENGI

Swali lililopo ni hili: Je Torati iliharimisha kuoa wake zaidi? Torati inasema, Akiwa mtu ana wake wawili, mmoja ampenda, mmoja hampendi, nao wamemzalia vijana . . . na yule mzaliwa wa kwanza akiwa ni wa mke asiyependwa; ndipo itakapokuwa ya kwamba siku atakayowarithisha wanawe alivyo navyo, na asimweke mwana wa ampendaye kuwa mzaliwa wa kwanza mbele ya mwana wa asiyempenda," (Kumbukumbu 21:15-17). Pia soma Kumbukumbu 25:5. Je, maneno hayo hayaonyeshi kuwa kuoa zaidi hakulaumiwi? Ni wazi Wakristo wanapinza maneno ya Yesu aliyewaambia wafuate amri zote za Torati na maneno ya Manabii na ya Mashekhe wa Kiyahudi.

وَاٰتُوا النِّسَآءَ صَدُقٰتِهِنَّ نِحْلَةً ؕ فَاِنْ
طِبْنَ لَكُمْ عَنْ شَیْءٍ مِّنْهُ نَفْسًا فَكُلُوْهُ
هَنِیْٓـًٔا مَّرِیْٓـًٔا ۝۵

5. Na wapeni wanawake mahari zao kwa dhati ya moyo. Lakini wakiwapeni cho chote kwa radhi ya nafsi zao katika hayo, basi kileni kwa furaha bila ya kusita.

وَلَا تُؤْتُوا السُّفَهَآءَ اَمْوَالَكُمُ الَّتِیْ جَعَلَ
اللّٰهُ لَكُمْ قِیٰمًا وَّارْزُقُوْهُمْ فِیْهَا
وَاكْسُوْهُمْ وَقُوْلُوْا لَهُمْ قَوْلًا مَّعْرُوْفًا ۝۶

6. Wala msiwape mamlaka ya kuzitunza mali zenu ambazo Allah Amezifanya kuwa ndiyo njia yenu ya kujikimu, wale ambao hawana uwezo kiakili wa kumiliki mali. Kwa hiyo walisheni na wavisheni vizuri tu na mseme nao kwa kauli njema.

Zaidi ya hayo Biblia inaeleza ya kuwa Nabii Ibrahimu alikuwa na wake wawili, Sara na Hajira (Mwanzo 16:1-2); ya kwamba Nabii Yakubu aliposwa wake wawili, Leakh na Rakheli na akapewa wajakazi, Zilfa na Bilhah (Mwanzo 29:16-30); ya kwamba Nabii Daudi alikuwa na wake wengi na masuria (2 Samuel 12:8 na 15:16); ya kwamba Nabii Sulemani alikuwa na wake mia saba na masuria mia tatu (1 Wafalme 11:3). Kama kuoa wake wengi kungekuwa jambo ovu, ilikuwaje Torati, ambayo Yesu anahimiza sana ifuatwe, isilikataze?

HAIWEZEKANI KUIFUATA INJILI

Lakini kama tufuate Injili katika hukumu za ndoa, kwa vile si za kiasili, zitatuletea taabu nyingi za bure kama vile zinavyowasumbua Wakristo. Katika Ukristo, "waliojaliwa" ni wale wasiotaka kuoa. Imeandikwa, "Wanafunzi wake wakamwambia, Mambo ya mtu na mkewe ya-kiwa hivyo haifai kuoa. Lakini yeye akawaambia, si wote wawezao kulipokea neno hilo, ila wale waliojaliwa. Maana wako matowashi waliozaliwa hali hiyo toka matumboni mwa mama zao; tena wako matowashi waliojifanya kuwa matowashi kwa ajili ya ufalme wa mbinguni. Awezaye kulipokea neno hili na alipokee" (Matt. 19:10-12). Maneno haya yanaonyesha wazi ya kuwa waliojihasi kwa ajili ya dini, wao ndio Wakristo "waliojaliwa." Lakini kujaliwa huko kusiko kwa asili ya kibinadamu kumewashinda Wakristo karibu wote, na kadhalika kundi kubwa sana la mapadre limeshindwa kuwa wenye kujaliwa hivyo.

Bwana Paulo pia anafundisha kama hayo na kusema, "Ni heri mwanamume asiguse mwa-namke. Lakini kwa sababu ya zinaa kila mwanamume na awe na mke wake mwenyewe. . .Lakin nawaambia wale wasiooa bado , na wajane, ni heri wakae kama mimi nilivyo. Lakini ikiwa hawawezi kujizuia, na waoe" (1 Wakorintho 7:1-7). Maneno haya yanazidi kubainisha kuwa bila kuoa ndiyo heri, na asiyeweza kufanya hivyo ndiye aoe. Tunamshukuru Allah aliyetia chuki ya fundisho hili katika nyoyo za watu, au sivyo dunia ingalikoma zamani, na mapadre wenyewe wasingeona mtu wa kumwambia "Ni heri usioe."

Wakristo wanasadiki ya kwamba amri ya Mungu kwa Adamu ni kuwa, "Zaeni, mwongezeke, mwijaze nchi" (Mwanzo 1:28); na kinyume cha amri hiyo Paulo anatuambia, "Ni heri mwanamume asimguse mwanamke" na ya kwamba kukaa bila kuoa ndilo jambo lenye heri. Sasa kama tutafuata maagizo hayo ya Paulo, amri hiyo ya Mungu, "Zaeni, mwongezeke, mwijaze nchi" itakuwa vizuri kuivunja?

Aya 5. *Wapeni wanawake mahari zao kwa hiba,* pia maneno haya yanaonyesha kiasi cha mahari kiwe cha maana, yaani, ambacho mume anaweza kukitoa bila taabu, na kwa furaha.

Aya 6. *Sufahaau,* "Wapumbavu." Neno hili maana yake hasa ni "watu wasioweza kuan-galia vizuri mali zao," na limetumiwa badala ya neno "yatima" ili liwe na maana pana zaidi na lipate kuwahusu watu wengine.

وَابْتَلُوا الْيَتٰمٰى حَتّٰٓى اِذَا بَلَغُوا النِّكَاحَ ۚ
فَاِنْ اٰنَسْتُمْ مِّنْهُمْ رُشْدًا فَادْفَعُوْٓا
اِلَيْهِمْ اَمْوَالَهُمْ ۚ وَلَا تَاْكُلُوْهَآ اِسْرَافًا
وَّبِدَارًا اَنْ يَّكْبَرُوْا ۭ وَمَنْ كَانَ غَنِيًّا
فَلْيَسْتَعْفِفْ ۚ وَمَنْ كَانَ فَقِيْرًا فَلْيَاْكُلْ
بِالْمَعْرُوْفِ ۭ فَاِذَا دَفَعْتُمْ اِلَيْهِمْ
اَمْوَالَهُمْ فَاَشْهِدُوْا عَلَيْهِمْ ۭ وَكَفٰى بِاللّٰهِ
حَسِيْبًا ۝۶

7. Na wajaribuni mayatima mpaka wafikie umri wa kuoa; basi kama mkiwaona wana akili njema, muwape mali zao; wala msizile kwa pupa na kwa haraka kwa kuchelea watakuwa wakubwa. Na mwenye kuwa tajiri, basi ajiepushe; na aliye fukara basi azile kwa sheria. Na mtakapowapa mali zao, basi mwawekee mashahidi. Na Allah Anatosha kwa kufanya hesabu.

لِلرِّجَالِ نَصِيْبٌ مِّمَّا تَرَكَ الْوَالِدٰنِ
وَالْاَقْرَبُوْنَ ۠ وَلِلنِّسَاۗءِ نَصِيْبٌ مِّمَّا
تَرَكَ الْوَالِدٰنِ وَالْاَقْرَبُوْنَ مِمَّا قَلَّ مِنْهُ
اَوْ كَثُرَ ۭ نَصِيْبًا مَّفْرُوْضًا ۝۷

8. Wanaume wana sehemu katika yale waliyoyaacha wazazi na jamaa wa karibu; na wanawake (pia) wanayo sehemu katika yale waliyoyaacha wazazi na jamaa waliowakaribia, yakiwa kidogo au mengi: sehemu iliyofaradhiwa.

وَاِذَا حَضَرَ الْقِسْمَةَ اُولُوا الْقُرْبٰى
وَالْيَتٰمٰى وَالْمَسٰكِيْنُ فَارْزُقُوْهُمْ مِّنْهُ
وَقُوْلُوْا لَهُمْ قَوْلًا مَّعْرُوْفًا ۝۸

9. Na watakapohudhuria wakati wa kugawanya (mirathi), ndugu na yatima na maskini, basi wapeni katika hayo, na waambieni kauli njema.

Hapa inayoambiwa ni jamii nzima kwa pamoja ambapo mali inayozungumziwa si mali ya taifa bali ni ile ya mayatima ambao idadi yao huongezeka na kuwa kubwa sana wakati wa vita. Ni dhairi kwamba sehemu kubwa kidogo ya mali ya taifa itahusika katika mazingira yasiyokuwa ya kawaida ya namna hiyo. Kama taifa katika ujumla wake halitaitunza mali ya nama hiyo na kuiacha moja kwa moja chini ya uangalizi wa watoto wasiokuwa na uzoefu na wasiokuwa na uwezo wa kutunza mali zao kwa kutumia akili, kitendo hiki ni lazima kabisa kitaleta athari mbaya katika uchumi wote wa taifa. Ili kuliondoa tatizo hili, taifa linaambiwa katika ujumla wake na kupewa jukumu la kuitunza mali husika kana kwamba ni mali yao. Lakini hii haina maana kwamba mayatima wa namna hiyo hawatarithishwa au kwamba watanyang'anywa haki zao za kibinafsi moja kwa moja. Aya inayofuatia na aya ya 11 zinatoa maana halisi ya aya hii kwa uwazi sana.

Aya 7. *Tajiri, basi ajiepushe*. Aya hii ni tafsiri ya Aya 3 ya sura hii; inazidi kubainisha kuwa tajiri anayewalinda mayatima asichukue ujira katika mali zao; na maskini ameruhusiwa kulipwa sawa na kazi anayoifanya.

Aya 8. Aya hii ndiyo msingi wa kanuni ya Kiislamu ya urithi, na inaeleza kanuni ya haki za mwanamume na mwanamke, ya kuwa wote wana haki ya kupata sehemu katika mali ya urithi.

Aya 9. Ndugu waliotajwa katika Aya hii ni wale wasiokuwa na sehemu katika urithi. Aya hii inawapendelea Waislamu, wanapofanya wasia, wausie sehemu ya mali yao isiyozidi thuluthi moja kwa ajili ya kupewa ndugu wengine wasio na mafungu na mayatima na maskini.

وَلْيَخْشَ الَّذِيْنَ لَوْ تَرَكُوْا مِنْ خَلْفِهِمْ
ذُرِّيَّةً ضِعٰفًا خَافُوْا عَلَيْهِمْ ۠ فَلْيَتَّقُوا
اللّٰهَ وَلْيَقُوْلُوْا قَوْلًا سَدِيْدًا ۝٩

10. Na watu hao waogope kama wangeacha nyuma yao wazao wadhaifu wangekuwa na hofu juu yao; basi wamwogope Allah na waseme kauli iliyo sawa.

اِنَّ الَّذِيْنَ يَاْكُلُوْنَ اَمْوَالَ الْيَتٰمٰى
ظُلْمًا اِنَّمَا يَاْكُلُوْنَ فِيْ بُطُوْنِهِمْ نَارًا ؕ
وَسَيَصْلَوْنَ سَعِيْرًا ۝١٠ ع ١١/١٢

11. Hakika wale wanaokula mali ya yatima kwa dhuluma, bila shaka wanakula moto matumboni mwao; na hivi karibuni wataungua katika moto uwakao.

FUNGU 2

يُوْصِيْكُمُ اللّٰهُ فِيْٓ اَوْلَادِكُمْ ۗ لِلذَّكَرِ
مِثْلُ حَظِّ الْاُنْثَيَيْنِ ۚ فَاِنْ كُنَّ نِسَآءً
فَوْقَ اثْنَتَيْنِ فَلَهُنَّ ثُلُثَا مَا تَرَكَ ۚ وَاِنْ
كَانَتْ وَاحِدَةً فَلَهَا النِّصْفُ ؕ وَلِاَبَوَيْهِ
لِكُلِّ وَاحِدٍ مِّنْهُمَا السُّدُسُ مِمَّا تَرَكَ
اِنْ كَانَ لَهٗ وَلَدٌ ۚ فَاِنْ لَّمْ يَكُنْ لَّهٗ وَلَدٌ
وَّوَرِثَهٗٓ اَبَوٰهُ فَلِاُمِّهِ الثُّلُثُ ۚ فَاِنْ كَانَ
لَهٗٓ اِخْوَةٌ فَلِاُمِّهِ السُّدُسُ مِنْۢ بَعْدِ وَصِيَّةٍ
يُّوْصِيْ بِهَآ اَوْ دَيْنٍ ؕ اٰبَآؤُكُمْ
وَاَبْنَآؤُكُمْ لَا تَدْرُوْنَ اَيُّهُمْ اَقْرَبُ
لَكُمْ نَفْعًا ؕ فَرِيْضَةً مِّنَ اللّٰهِ ؕ اِنَّ اللّٰهَ
كَانَ عَلِيْمًا حَكِيْمًا ۝١١

12. Allah Anawausieni juu ya watoto wenu; mwanamume apate sawa na sehemu ya wanawake wawili; na wakiwa wanawake zaidi ya wawili, basi watapata thuluthi mbili za (mali) aliyoacha; lakini akiwa mmoja basi apewe nusu. Na wazazi wake wawili, kila mmoja wao apate sehemu ya sita ya (mali) aliyoacha, akiwa (yule marehemu) anaye mtoto; lakini kama hana mtoto, na wazazi wake wawili wamekuwa ndio warithi wake, basi mama yake atapata thuluthi moja, na kama (marehemu) anao ndugu, basi mama yake atapata sehemu ya sita, baada ya kutoa wasia aliouusia au kulipa deni. Baba zenu na watoto wenu: ninyi hamjui ni nani miongoni mwao aliye karibu zaidi kuwafaidisheni. Hiyo ni sheria iliyotoka kwa Allah. Bila shaka Allah ni Mjuzi, Mwenye hekima.

Aya 12. Aya hii na inayofuata zinaeleza hukumu za urithi kwa muhtasari. Dini ya Kiislamu imewawekea sehemu za urithi ndugu wote wa karibu wa mtu aliyefariki, wake kwa waume, bila kufuata walivyofuatana katika kuzaliwa. Watoto, wazazi, waume, wake, wanapokuwa hai, hupata sehemu zao, katika kila hali, na ndugu wengine hupata sehemu katika matukio maalum. Mwanamume amepewa sehemu mbili kuliko mwanamke maana yeye anayo madaraka ya kuwapa matumizi watu wa nyumbani mwake (Ma'aani jalada 2 uk. 32).

13. Na ninyi mtapata nusu ya (mali) walizoziacha wake zenu, kama wao hawana mtoto; na ikiwa wana mtoto, ninyi mtapata robo ya walivyoacha, baada ya kutoa wasia waliouusia au kulipa deni. Nao (wake zenu) watapata robo ya mlivyoacha, ikiwa hamna mtoto; lakini kama mnaye mtoto, basi wao watapata sehemu ya nane ya vile mlivyoacha, baada ya kutoa wasia mliouusia au kulipa deni. Na kama mwanamume au mwanamke anayerithiwa hana mtoto wala wazazi, lakini anaye kaka au dada, basi kila mmoja wa hawa atapata sehemu ya sita; Lakini kama wakiwa zaidi kuliko hao basi wagawane hisa zilizo sawa katika theluthi moja baada ya kutoa wasia waliouusia au kulipa deni, bila ya kumdhuru ye yote. Huu ni wasia kutoka kwa Allah; na Allah ni Mjuzi, Mpole sana.

14. Hiyo ni mipaka ya Allah; na anayemtii Allah na Mtume Wake, Yeye Atamwingiza katika Bustani zipitazo mito ndani yake; watakaa humo milele na huo ndio ufaulu mkuu.

وَلَكُمْ نِصْفُ مَا تَرَكَ أَزْوَاجُكُمْ إِنْ
لَّمْ يَكُنْ لَّهُنَّ وَلَدٌ ۚ فَإِنْ كَانَ لَهُنَّ وَلَدٌ
فَلَكُمُ الرُّبُعُ مِمَّا تَرَكْنَ مِنْ بَعْدِ وَصِيَّةٍ
يُوصِينَ بِهَا أَوْ دَيْنٍ ۗ وَلَهُنَّ الرُّبُعُ مِمَّا
تَرَكْتُمْ إِنْ لَّمْ يَكُنْ لَّكُمْ وَلَدٌ ۚ فَإِنْ كَانَ
لَكُمْ وَلَدٌ فَلَهُنَّ الثُّمُنُ مِمَّا تَرَكْتُمْ مِّنْ
بَعْدِ وَصِيَّةٍ تُوصُونَ بِهَا أَوْ دَيْنٍ ۗ وَإِنْ
كَانَ رَجُلٌ يُّورَثُ كَلٰلَةً أَوِ امْرَأَةٌ وَّلَهٗ
أَخٌ أَوْ أُخْتٌ فَلِكُلِّ وَاحِدٍ مِّنْهُمَا
السُّدُسُ ۚ فَإِنْ كَانُوْٓا أَكْثَرَ مِنْ ذٰلِكَ
فَهُمْ شُرَكَآءُ فِي الثُّلُثِ مِنْ بَعْدِ وَصِيَّةٍ
يُّوصٰى بِهَآ أَوْ دَيْنٍ ۙ غَيْرَ مُضَآرٍّ ۚ
وَصِيَّةً مِّنَ اللّٰهِ ۗ وَاللّٰهُ عَلِيْمٌ حَلِيْمٌ ﴿١٣﴾
تِلْكَ حُدُوْدُ اللّٰهِ ۗ وَمَنْ يُّطِعِ اللّٰهَ
وَرَسُوْلَهٗ يُدْخِلْهُ جَنّٰتٍ تَجْرِيْ مِنْ
تَحْتِهَا الْأَنْهٰرُ خٰلِدِيْنَ فِيْهَا ۗ وَذٰلِكَ
الْفَوْزُ الْعَظِيْمُ ﴿١٤﴾

Aya imeeleza namna tatu za sehemu za wazazi: (1) Kama mtu amekufa na amewacha mtoto mmoja au zaidi, basi kila mzazi wake atapata 1/6; (2) kama mtu amekufa hana mtoto na wazazi wake peke yao ndio warithi, na hakuacha mke au mume, basi mama atapata 1/3 ya mali, na 2/3 zilizobaki atachukua baba; (3) mtu anakufa bila kuzaa, na wazazi wake peke yao ndio warithi wake, lakini marehemu huyo anao nduguze na dadaze, hapo, ingawa nduguze na dadaze hawatamrithi, lakini kuwapo kwao kutabadili mafungu ya wazazi; hapa mama atapata 1/6 (badala ya 1/3) na 5/6 zilizobaki zitakwenda kwa baba. Sababu ya baba kupewa sehemu kubwa zaidi hapa ni kwamba yeye ndiye anawapa matumizi ndugu na dada za marehemu.

Aya 13. *Kalaala,* "Hana mtoto wala mzazi." Neno *kalaala* lina maana hizi: (1) Mtu ambaye amekufa na hakuacha baba wala mtoto wa kiume au wa kike; au (2) mtu ambaye hakuacha baba wala mtoto wa kiume. Ibni Abbas anasema, *Kalaala* ni mtu asiyeacha mtoto wa kiume, haidhuru hata kama baba yake yu hai au amekufa, na hii ndiyo maana ya (3) ya neno *Kalaala* (Lane, Akrab na Mufradat).

15. Na anayemwasi Allah na Mtume Wake, na kuiruka mipaka Yake, Atamwingiza Motoni, humo atakaa, na atapata adhabu ifedheheshayo.

وَمَنْ يَّعْصِ اللّٰهَ وَ رَسُوْلَهٗ وَيَتَعَدَّ حُدُوْدَهٗ يُدْخِلْهُ نَارًا خَالِدًا فِيْهَا ۪ وَلَهٗ عَذَابٌ مُّهِيْنٌ ﴿١٥﴾ ع ١٣

FUNGU 3

16. Na wale wafanyao upujufu miongoni mwa wanawake wenu, basi mwaite mashahidi wanne juu yao miongoni mwenu; na kama wakishuhudia, basi mwazuie majumbani mpaka mauti iwafishe au Allah awafanyie njia nyingine.

وَالّٰتِيْ يَاْتِيْنَ الْفَاحِشَةَ مِنْ نِّسَآئِكُمْ فَاسْتَشْهِدُوْا عَلَيْهِنَّ اَرْبَعَةً مِّنْكُمْ ۚ فَاِنْ شَهِدُوْا فَاَمْسِكُوْهُنَّ فِي الْبُيُوْتِ حَتّٰى يَتَوَفّٰهُنَّ الْمَوْتُ اَوْ يَجْعَلَ اللّٰهُ لَهُنَّ سَبِيْلًا ﴿١٦﴾

17. Na wale (wanaume) wawili wanaoufanya (upujufu) miongoni mwenu, basi waadhibuni wote wawili; na kama wakitubia na kujisahihisha, basi waacheni; hakika Allah ndiye Apokeaye toba, Mwenye kurehemu.

وَالَّذٰنِ يَاْتِيٰنِهَا مِنْكُمْ فَاٰذُوْهُمَا ۚ فَاِنْ تَابَا وَاَصْلَحَا فَاَعْرِضُوْا عَنْهُمَا ؕ اِنَّ اللّٰهَ كَانَ تَوَّابًا رَّحِيْمًا ﴿١٧﴾

18. Toba inayopokelewa na Allah ni ya wale tu wanaofanya uovu kwa ujinga, kisha wakatubia papo kwa papo; basi hao ndio Allah Huipokea toba yao; na Allah ni Mjuzi, Mwenye hekima.

اِنَّمَا التَّوْبَةُ عَلَى اللّٰهِ لِلَّذِيْنَ يَعْمَلُوْنَ السُّوْٓءَ بِجَهَالَةٍ ثُمَّ يَتُوْبُوْنَ مِنْ قَرِيْبٍ فَاُولٰٓئِكَ يَتُوْبُ اللّٰهُ عَلَيْهِمْ ؕ وَكَانَ اللّٰهُ عَلِيْمًا حَكِيْمًا ﴿١٨﴾

19. Na si toba ya wale ambao hufanya maovu mpaka mauti imemhudhuria mmoja wao, husema: Hakika mimi sasa natubu; wala ya wale ambao wanakufa katika hali ya ukafiri. Hao ndio Tumewaandalia adhabu iumizayo.

وَلَيْسَتِ التَّوْبَةُ لِلَّذِيْنَ يَعْمَلُوْنَ السَّيِّاٰتِ ۚ حَتّٰٓى اِذَا حَضَرَ اَحَدَهُمُ الْمَوْتُ قَالَ اِنِّيْ تُبْتُ الْـٰٔنَ وَلَا الَّذِيْنَ يَمُوْتُوْنَ وَهُمْ كُفَّارٌ ؕ اُولٰٓئِكَ اَعْتَدْنَا لَهُمْ عَذَابًا اَلِيْمًا ﴿١٩﴾

Aya 16. Wanawake wanaotajwa hapa ni wale wanaoonekana na uasherati pasipo kuzini; ndivyo walivyofahamu Aya hii Abu Muslim na Mujahid na wengineo: yaani wanawake hao wazuiwe majumbani mwao wasichanganyike na wanawake wengine mpaka wameacha mwenendo mbaya au wameolewa. Na kwa kuwa kosa hili ni kubwa, basi ni lazima lishuhudiwe na mashahidi wanne ili wanawake wasidhulumiwe bure.

20. Enyi mlioamini, si halali kwenu kuwarithi wanawake kwa nguvu; wala msiwazuie (kuolewa) ili mpate kuwanyang'anya baadhi ya vile mlivyowapa, isipokuwa wawe wamefanya uovu ulio wazi; na kaeni nao kwa wema ; na kama mkiwachukia, basi huenda mchukie kitu na Allah Ametia heri nyingi ndani yake.

يٰٓاَيُّهَا الَّذِيْنَ اٰمَنُوْا لَا يَحِلُّ لَكُمْ اَنْ تَرِثُوا
النِّسَآءَ كَرْهًا ؕ وَلَا تَعْضُلُوْهُنَّ لِتَذْهَبُوْا
بِبَعْضِ مَآ اٰتَيْتُمُوْهُنَّ اِلَّآ اَنْ يَّاْتِيْنَ
بِفَاحِشَةٍ مُّبَيِّنَةٍ ۚ وَعَاشِرُوْهُنَّ بِالْمَعْرُوْفِ ۚ
فَاِنْ كَرِهْتُمُوْهُنَّ فَعَسٰٓى اَنْ تَكْرَهُوْا
شَيْـًٔا وَّيَجْعَلَ اللّٰهُ فِيْهِ خَيْرًا كَثِيْرًا ۝١٩

21. Na kama mkitaka kubadilisha mke mahali pa mke (wa zamani) na hali mmoja wao mmempa rundo la mali, basi msimnyang'anye cho chote. Je, mtainyang'anya kwa kusingizia na kwa hatia iliyo wazi?

وَاِنْ اَرَدْتُّمُ اسْتِبْدَالَ زَوْجٍ مَّكَانَ
زَوْجٍ ۙ وَّاٰتَيْتُمْ اِحْدٰىهُنَّ قِنْطَارًا فَلَا تَاْخُذُوْا
مِنْهُ شَيْـًٔا ؕ اَتَاْخُذُوْنَهٗ بُهْتَانًا وَّاِثْمًا مُّبِيْنًا ۝٢٠

22. Na mtainyang'anyaje na hali ninyi kwa ninyi mmeingiliana, nao wamepokea kwenu ahadi thabiti?

وَكَيْفَ تَاْخُذُوْنَهٗ وَقَدْ اَفْضٰى بَعْضُكُمْ
اِلٰى بَعْضٍ وَّاَخَذْنَ مِنْكُمْ مِّيْثَاقًا غَلِيْظًا ۝٢١

23. Wala msiwaoe wake waliowaoa baba zenu, isipokuwa yale yaliyokwisha pita. Bila shaka jambo hilo ni uovu na chukizo, na njia mbaya.

وَلَا تَنْكِحُوْا مَا نَكَحَ اٰبَآؤُكُمْ مِّنَ النِّسَآءِ
اِلَّا مَا قَدْ سَلَفَ ؕ اِنَّهٗ كَانَ فَاحِشَةً
وَّمَقْتًا ؕ وَسَآءَ سَبِيْلًا ۝٢٢ ع ٤/١٤

FUNGU 4

24. Mmeharimishiwa (kuoa) mama zenu, na binti zenu, na dada zenu, na shangazi zenu, na dada za mama zenu, na binti za ndugu, na binti za dada, na mama zenu waliowanyonyesheni, na dada zenu wa kunyonya, na mama za wake zenu, na binti zenu wa kambo walio katika ulinzi wenu, waliozaliwa na

حُرِّمَتْ عَلَيْكُمْ اُمَّهٰتُكُمْ وَبَنٰتُكُمْ
وَاَخَوٰتُكُمْ وَعَمّٰتُكُمْ وَخٰلٰتُكُمْ وَبَنٰتُ
الْاَخِ وَبَنٰتُ الْاُخْتِ وَاُمَّهٰتُكُمُ الّٰتِيْٓ
اَرْضَعْنَكُمْ وَاَخَوٰتُكُمْ مِّنَ الرَّضَاعَةِ
وَاُمَّهٰتُ نِسَآئِكُمْ وَرَبَآئِبُكُمُ الّٰتِيْ فِيْ
حُجُوْرِكُمْ مِّنْ نِّسَآئِكُمُ الّٰتِيْ دَخَلْتُمْ

Aya 21. Sio mradi wa Aya hii kuwa mtu anayo ruhusa ya kumwacha mkewe bure. Lazima pawe na sababu za kutosha. Mtume *s.a.w.* alisema: "Hakika jambo la halali linalochukiza sana mbele ya Allah ni talaka" (Dawud, sura ya *Talaak*).

Aya 23. *Isipokuwa yale yaliyokwisha pita.* Yaani waliofanya kosa la kuoa wanawake walioharimishwa walipokuwa hawajawa Waislamu, wao watasamehewa; lakini ni lazima wawaache wanawake hao mara moja.

wake zenu mliowaingilia lakini kama ninyi hamjawaingilia, basi si vibaya kwenu (kuwaoa) na wake wa wana wenu waliotoka katika migongo yenu; na pia (imeharamishwa) ya kwamba mwaoe madada wawili wakati mmoja, isipokuwa yale yaliyokwisha pita; hakika Allah ndiye Msamehevu, Mrehemevu.

بِهِنَّ ۗ فَاِنْ لَّمْ تَكُوْنُوْا دَخَلْتُمْ بِهِنَّ فَلَا
جُنَاحَ عَلَيْكُمْ ۗ وَحَلَآئِلُ اَبْنَآئِكُمُ
الَّذِيْنَ مِنْ اَصْلَابِكُمْ ۙ وَاَنْ تَجْمَعُوْا بَيْنَ
الْاُخْتَيْنِ اِلَّا مَا قَدْ سَلَفَ ۗ اِنَّ اللّٰهَ كَانَ
غَفُوْرًا رَّحِيْمًا ﴿٢٤﴾

JUZU 5

25. Na pia (mmeharamishiwa) wanawake wenye kuolewa, isipokuwa wale iliyowamiliki mikono yenu ya kuume. Ndiyo sheria ya Allah juu yenu. Na mmehalalishiwa (kuoa wanawake) minghairi ya hao, kwamba mwatafute kwa mali zenu, kwa kuwaoa bila ya kufanya zinaa, Na kwa ajili ya faida mnayoipata kwao, basi wapeni mahari zao zilizolazimishwa; wala si vibaya kwenu katika yale mli yoridhiana baada ya (kutoa) mahari. Hakika Allah ni Mjuzi, Mwenye hekima.

وَّالْمُحْصَنٰتُ مِنَ النِّسَآءِ اِلَّا مَا
مَلَكَتْ اَيْمَانُكُمْ ۚ كِتٰبَ اللّٰهِ عَلَيْكُمْ ۚ
وَاُحِلَّ لَكُمْ مَّا وَرَآءَ ذٰلِكُمْ اَنْ تَبْتَغُوْا
بِاَمْوَالِكُمْ مُّحْصِنِيْنَ غَيْرَ مُسٰفِحِيْنَ ۗ
فَمَا اسْتَمْتَعْتُمْ بِهٖ مِنْهُنَّ فَاٰتُوْهُنَّ
اُجُوْرَهُنَّ فَرِيْضَةً ۗ وَلَا جُنَاحَ عَلَيْكُمْ
فِيْمَا تَرٰضَيْتُمْ بِهٖ مِنْۢ بَعْدِ الْفَرِيْضَةِ ۗ
اِنَّ اللّٰهَ كَانَ عَلِيْمًا حَكِيْمًا ﴿٢٥﴾

26. Na miongoni mwenu asiyeweza kupata mali ya kuoa wanawake waungwana, waaminio, basi (aoe) katika wajakazi waaminio iliyowamiliki mikono yenu ya kuume, na Allah Anaijua sana imani yenu;

وَمَنْ لَّمْ يَسْتَطِعْ مِنْكُمْ طَوْلًا اَنْ يَّنْكِحَ
الْمُحْصَنٰتِ الْمُؤْمِنٰتِ فَمِنْ مَّا مَلَكَتْ
اَيْمَانُكُمْ مِّنْ فَتَيٰتِكُمُ الْمُؤْمِنٰتِ ۗ وَاللّٰهُ
اَعْلَمُ بِاِيْمَانِكُمْ ۗ بَعْضُكُمْ مِّنْۢ
بَعْضٍ ۚ فَانْكِحُوْهُنَّ بِاِذْنِ اَهْلِهِنَّ

Aya 25. *Muhsanaat,* "Wanawake wenye kuolewa," pia wamekatazwa kuolewa na mtu mwingine, yaani, ni haramu mtu kumwoa mke wa mtu mwingine. Neno *Muhsanaat* pia limetumika katika Qur'an kwa maana hizi, (1) mwanamke mtawa na (2) mwanamke ambaye si mtumwa. (lane na Akrab).

Iliyowamiliki mikono yenu ya kuume, yaani wanawake waliotekwa katika vita iliyoletwa na maadui kwa kutaka kuuvunja Uislamu. Sababu ya kutolewa ruhusa ya kuwaoa ni kwamba wapate raha.

وَاٰتُوْهُنَّ اُجُوْرَهُنَّ بِالْمَعْرُوْفِ
مُحْصَنٰتٍ غَيْرَ مُسٰفِحٰتٍ وَّلَا مُتَّخِذٰتِ
اَخْدَانٍ ۚ فَاِذَآ اُحْصِنَّ فَاِنْ اَتَيْنَ
بِفَاحِشَةٍ فَعَلَيْهِنَّ نِصْفُ مَا عَلَى
الْمُحْصَنٰتِ مِنَ الْعَذَابِ ؕ ذٰلِكَ لِمَنْ خَشِيَ
الْعَنَتَ مِنْكُمْ ؕ وَاَنْ تَصْبِرُوْا خَيْرٌ
لَّكُمْ ؕ وَاللّٰهُ غَفُوْرٌ رَّحِيْمٌ ﴿٢٦﴾ ع ٤

m-ninyi kwa ninyi, basi mwaoe kwa idhini ya mabwana wao na wapeni mahari zao kwa sheria, wanawake wema, wasio waasherati, wala wenye kushika mahawara. Na wanapoolewa kisha wakafanya ufasiki, basi itakuwa adhabu juu yao nusu ya adhabu iliyowekwa kwa wanawake waungwana. Hayo ni kwa yule miongoni mwenu anayeogopa kupata udhia. Na ya kwamba msubiri ndiyo bora kwenu. Na Allah ni Msamehevu, Mrehemevu.

FUNGU 5

يُرِيْدُ اللّٰهُ لِيُبَيِّنَ لَكُمْ وَيَهْدِيَكُمْ سُنَنَ
الَّذِيْنَ مِنْ قَبْلِكُمْ وَيَتُوْبَ عَلَيْكُمْ ؕ
وَاللّٰهُ عَلِيْمٌ حَكِيْمٌ ﴿٢٧﴾

27. Allah Anataka kuwabainishieni na kuwaongozeni kwenye mwenendo wa wale waliowatangulieni, na kuwaelekeeni (kwa rehema Yake); na Allah ni Mjuzi, Mwenye hekima.

وَاللّٰهُ يُرِيْدُ اَنْ يَّتُوْبَ عَلَيْكُمْ ۖ وَيُرِيْدُ
الَّذِيْنَ يَتَّبِعُوْنَ الشَّهَوٰتِ اَنْ تَمِيْلُوْا
مَيْلًا عَظِيْمًا ﴿٢٨﴾

28. Na Allah Anataka kuwaelekeeni (kwa rehema Yake); lakini wanaofuata matamanio (yao) hutaka ya kwamba mgeuke mgeuko mkubwa.

يُرِيْدُ اللّٰهُ اَنْ يُّخَفِّفَ عَنْكُمْ ۚ وَخُلِقَ
الْاِنْسَانُ ضَعِيْفًا ﴿٢٩﴾

29. Allah Anataka kuwapunguzieni, maana mwanadamu ameumbwa dhaifu.

Ikumbukwe kwamba Islam hairuhusu kuteka wanawake katika vita zingine za desturi. Hapa iliruhusiwa ili kulipiza kisasi kwa maadui waliowateka wanawake wa Kiislamu na kuwafanya watumwa. Hatua hii pia ilikusudiwa kuzuia ufisadi ambao mara nyingi hutokea katika hali za namna hii. soma sura 24:34.

Aya 29. *Allah Anataka kuwapunguzieni.* Mwanadamu ni mwanadamu, hakukamilika. Hivyo asingeweza kutunga Sheria kamili ya kumfaa. Ili kumpunguzia taabu, Allah Mwenyewe amemtengenezea kanuni zote zilizo muhimu zipate kumwongoza. Hapa ni dhahiri Sheria imekuwa rehema kwa ajili ya watu, mbali na vile wanavyodhani Wakristo kuwa "Sheria ni laana." (Wagalatia 3:13).

30. Enyi mlioamini, msiliane mali zenu kwa ubatili, isipokuwa iwe biashara kwa kuridhiana kati yenu; wala msijiue nafsi zenu; hakika Allah ni Mwenye kuwahurumieni.

يٰٓاَيُّهَا الَّذِيْنَ اٰمَنُوْا لَا تَاْكُلُوْٓا اَمْوَالَكُمْ بَيْنَكُمْ بِالْبَاطِلِ اِلَّآ اَنْ تَكُوْنَ تِجَارَةً عَنْ تَرَاضٍ مِّنْكُمْ ۣ وَلَا تَقْتُلُوْٓا اَنْفُسَكُمْ ۭ اِنَّ اللّٰهَ كَانَ بِكُمْ رَحِيْمًا ۝۲۹

31. Na atakayefanya hivi kwa uadui na dhuluma, basi kwa yakini huyo Tutamwingiza Motoni; na hayo ni rahisi kwa Allah.

وَمَنْ يَّفْعَلْ ذٰلِكَ عُدْوَانًا وَّظُلْمًا فَسَوْفَ نُصْلِيْهِ نَارًا ۭ وَكَانَ ذٰلِكَ عَلَي اللّٰهِ يَسِيْرًا ۝۳۰

32. Kama mkijiepusha na maovu makubwa mnayokatazwa, Tutawafutieni makosa yenu na Tutawaingizeni mahali patukufu.

اِنْ تَجْتَنِبُوْا كَبَاۗىِٕرَ مَا تُنْهَوْنَ عَنْهُ نُكَفِّرْ عَنْكُمْ سَيِّاٰتِكُمْ وَنُدْخِلْكُمْ مُّدْخَلًا كَرِيْمًا ۝۳۱

33. Wala msitamani vile ambavyo Allah Amewafadhili baadhi yenu kuliko wengine. Wanaume wanayo sehemu ya vile walivyovichuma, na wanawake wanayo sehemu ya vile walivyovichuma. Na mwombeni Allah fadhili Zake, hakika Allah ni Mjuzi wa kila kitu.

وَلَا تَتَمَنَّوْا مَا فَضَّلَ اللّٰهُ بِهٖ بَعْضَكُمْ عَلٰي بَعْضٍ ۭ لِلرِّجَالِ نَصِيْبٌ مِّمَّا اكْتَسَبُوْا ۭ وَلِلنِّسَاۗءِ نَصِيْبٌ مِّمَّا اكْتَسَبْنَ ۭ وَسْـَٔـلُوا اللّٰهَ مِنْ فَضْلِهٖ ۭ اِنَّ اللّٰهَ كَانَ بِكُلِّ شَيْءٍ عَلِيْمًا ۝۳۲

34. Na kila (mtu) tumemwekea warithi wa yale waliyoyaacha wazazi wawili na ndugu zake; na wale mnaofungamana nao ahadi, basi wapeni sehemu yao; hakika Allah ni shahidi wa kila kitu.

وَلِكُلٍّ جَعَلْنَا مَوَالِيَ مِمَّا تَرَكَ الْوَالِدٰنِ وَالْاَقْرَبُوْنَ ۭ وَالَّذِيْنَ عَقَدَتْ اَيْمَانُكُمْ فَاٰتُوْهُمْ نَصِيْبَهُمْ ۭ اِنَّ اللّٰهَ كَانَ عَلٰي كُلِّ شَيْءٍ شَهِيْدًا ۝۳۳ ع

Aya 30. *Msijiue nafsi zenu.* Mtume *s.a.w.* amesema; "Mtu anayejiua kwa silaha, ataletwa siku ya Hukumu pamoja na silaha ile mkononi mwake na atatupwa Motoni na humo atakaa. Na mtu atakayejiua kwa sumu atatupwa ndani ya Moto pamoja na sumu ile, na humo ataendelea kuila" (Kathir).

Aya 33. *Wala msitamani,* yaani (1) mtu asiombe ya kuwa Mungu ampe kitu kile kile alicho nacho mwenzake, yaani yule mwenye nacho akinyang'anywe kihamie kwake; (2) mtu anaweza kuomba apewe kitu kama alichonacho mwenzake; (3) mtu anapoomba asiweke mbele yake mtu fulani aliyefadhiliwa, akitamani kuwa Mungu amfanyie kama alivyomfanyia mtu yule. Hii ni kama kuuwekea kipimo uwezo wa Allah. Mtu aombe tu kwa Allah afadhiliwe maana fadhili za Mungu hazina kipimo.

FUNGU 6

اَلرِّجَالُ قَوّٰمُوْنَ عَلَى النِّسَآءِ بِمَا فَضَّلَ
اللّٰهُ بَعْضَهُمْ عَلٰى بَعْضٍ وَّ بِمَآ اَنْفَقُوْا
مِنْ اَمْوَالِهِمْ ؕ فَالصّٰلِحٰتُ قٰنِتٰتٌ
حٰفِظٰتٌ لِّلْغَيْبِ بِمَا حَفِظَ اللّٰهُ ؕ
وَالّٰتِيْ تَخَافُوْنَ نُشُوْزَهُنَّ فَعِظُوْهُنَّ
وَاهْجُرُوْهُنَّ فِي الْمَضَاجِعِ وَاضْرِبُوْهُنَّ ۚ
فَاِنْ اَطَعْنَكُمْ فَلَا تَبْغُوْا عَلَيْهِنَّ سَبِيْلًا ؕ
اِنَّ اللّٰهَ كَانَ عَلِيًّا كَبِيْرًا ۝٣٤

35. Wanaume ni walinzi wa wanawake kwa sababu Allah amewafadhili baadhi yao kuliko wengine, na kwa sababu ya mali zao wanazozitoa; basi wanawake wema ni wale wenye kutii, wanaohifadhi (hata) wasipokuwapo (waume zao) yale Aliyohifadhi Allah. Na (wanawake) ambao mnaogopa uasi wao, basi waonyeni na waacheni peke yao katika vitanda, na wapigeni. Na kama wanawatii, basi msiwatafutie njia. Hakika Allah ndiye Aliye juu, Mkuu.

وَاِنْ خِفْتُمْ شِقَاقَ بَيْنِهِمَا فَابْعَثُوْا حَكَمًا
مِّنْ اَهْلِهٖ وَ حَكَمًا مِّنْ اَهْلِهَا ۚ
اِنْ يُّرِيْدَآ اِصْلَاحًا يُّوَفِّقِ اللّٰهُ بَيْنَهُمَا ؕ
اِنَّ اللّٰهَ كَانَ عَلِيْمًا خَبِيْرًا ۝٣٥

36. Na kama mkihofia uvunjaji wa ahadi ya ndoa baina yao, basi teueni mpatanishi mmoja kutoka katika jamaa za mwanamume na mpatanishi mmoja kutoka katika jamaa za mwanamke. Kama wote wawili wakitaka mapatano, Allah Atasababisha maafikiano yawepo baina yao. Hakika Allah ni Mjuzi, Mwenye habari.

وَاعْبُدُوا اللّٰهَ وَلَا تُشْرِكُوْا بِهٖ شَيْـًٔا
وَّبِالْوَالِدَيْنِ اِحْسَانًا وَّبِذِي الْقُرْبٰى
وَالْيَتٰمٰى وَالْمَسٰكِيْنِ وَالْجَارِ ذِي الْقُرْبٰى
وَالْجَارِ الْجُنُبِ وَالصَّاحِبِ بِالْجَنْۢبِ
وَابْنِ السَّبِيْلِ ۙ وَمَا مَلَكَتْ اَيْمَانُكُمْ ؕ
اِنَّ اللّٰهَ لَا يُحِبُّ مَنْ كَانَ مُخْتَالًا فَخُوْرَا ۝٣٦ ۙ

37. Na mwabuduni Allah wala msimshirikishe na cho chote, na wafanyieni hisani wazazi na pia jamaa za ukoo, na mayatima na maskini na jirani miongoni mwa jamaa, na jirani ambaye si jamaa, na rafiki aliye kando (yako), na msafiri, na wale iliyowamiliki mikono yenu ya kuume; bila shaka Allah Hampendi Mwenye kiburi, ajivunaye.

Aya 35. *Wapigeni.* Mwanamke anaweza kuadhibiwa na mumewe, lakini mifupa yake isijeruhiwe kamwe, na kipigo kisiwe cha kutia alama katika mwili wake (Tirmidhi, sura *Ridhaa*). Haya yote yamewekwa kwa ajili ya mwendo wa ufisadi ulio wazi. Mume hana haki kumwadhibu mkewe kwa makosa ya kawaida ya nyumbani au kwa kutoangalia kazi.

Aya 36. Tunafikiri kwamba si lazima kutumia neno "wapatanishi" kwa sababu kijina 'hao' chaweza kuwarejea pia wale wahusika wawili.

الَّذِيْنَ يَبْخَلُوْنَ وَيَاْمُرُوْنَ النَّاسَ بِالْبُخْلِ
وَيَكْتُمُوْنَ مَآ اٰتٰىهُمُ اللّٰهُ مِنْ فَضْلِهٖ ؕ
وَاَعْتَدْنَا لِلْكٰفِرِيْنَ عَذَابًا مُّهِيْنًا ﴿۳۸﴾

38. Ambao hufanya ubahili na huwaamuru watu kufanya ubahili, na kuyaficha Aliyowapa Allah kwa fadhili Zake. Na Tumewaandalia makafiri adhabu ifedheheshayo.

وَالَّذِيْنَ يُنْفِقُوْنَ اَمْوَالَهُمْ رِئَآءَ النَّاسِ
وَلَا يُؤْمِنُوْنَ بِاللّٰهِ وَلَا بِالْيَوْمِ الْاٰخِرِ ؕ
وَمَنْ يَّكُنِ الشَّيْطٰنُ لَهٗ قَرِيْنًا فَسَآءَ قَرِيْنًا ﴿۳۹﴾

39. Na ambao wanatoa mali zao kwa kuonyesha watu wala hawamwamini Allah wala siku ya Mwisho. Na yule mwenye kuwa Shetani rafiki yake, basi yeye ni rafiki mbaya sana.

وَمَاذَا عَلَيْهِمْ لَوْ اٰمَنُوْا بِاللّٰهِ وَالْيَوْمِ
الْاٰخِرِ وَاَنْفَقُوْا مِمَّا رَزَقَهُمُ اللّٰهُ ؕ
وَكَانَ اللّٰهُ بِهِمْ عَلِيْمًا ﴿۴۰﴾

40. Na ingekuwa nini juu yao kama wangelimwamini Allah na siku ya Mwisho, na kutoa katika yale Aliyowapa Allah? Na Allah Anawajua sana.

اِنَّ اللّٰهَ لَا يَظْلِمُ مِثْقَالَ ذَرَّةٍ ۚ وَاِنْ
تَكُ حَسَنَةً يُّضٰعِفْهَا وَيُؤْتِ مِنْ لَّدُنْهُ
اَجْرًا عَظِيْمًا ﴿۴۱﴾

41. Hakika Allah Hadhulumu (hata sawa na) uzito wa chembe; na kama likiwa ni tendo jema, Yeye Atalizidisha na kutoa ujira mkubwa kutoka Kwake.

فَكَيْفَ اِذَا جِئْنَا مِنْ كُلِّ اُمَّةٍۭ بِشَهِيْدٍ
وَّجِئْنَا بِكَ عَلٰى هٰٓؤُلَآءِ شَهِيْدًا ﴿۴۲﴾ ؕ

42. Basi itakuwaje tutakapoleta shahidi katika kila umati, na Tutakuleta wewe uwe shahidi juu ya hawa?

يَوْمَئِذٍ يَّوَدُّ الَّذِيْنَ كَفَرُوْا وَعَصَوُا
الرَّسُوْلَ لَوْ تُسَوّٰى بِهِمُ الْاَرْضُ ؕ
وَلَا يَكْتُمُوْنَ اللّٰهَ حَدِيْثًا ﴿۴۳﴾ ع

43. Siku hiyo watapenda walioukufuru na kumwasi Mtume ya kuwa laiti ardhi isawazishwe juu yao, wala hawatamficha Allah hadithi yo yote.

FUNGU 7

يٰٓاَيُّهَا الَّذِيْنَ اٰمَنُوْا لَا تَقْرَبُوا الصَّلٰوةَ
وَاَنْتُمْ سُكٰرٰى حَتّٰى تَعْلَمُوْا مَا تَقُوْلُوْنَ
وَلَا جُنُبًا اِلَّا عَابِرِيْ سَبِيْلٍ حَتّٰى

44. Enyi mlioamini, msiikaribie sala hali mmelewa mpaka muwe mnajua waziwazi mnayoyasema, wala katika hali ya janaba, isipokuwa mmo safarini, mpaka mwoge. Na kama mkiwa

Aya 44. *Hali mmelewa*. Sio mradi wake kulewa ulevi, maana ulevi umeharimishwa katika Uislamu. Kulewa huku ni kwa mtu kukosa kufahamu anayoyasema kama ilivyoeleza Aya yenyewe, yaani kama mtu anakuwa na njaa au hasira au usingizi na mengineyo (Bukhari, Abu Dawud).

Tayamamuni kwa udongo. Udongo umechaguliwa badala ya maji kwa sababu, kama vile maji

wagonjwa au safarini au mmoja wenu ametoka msalani au mmewagusa wanawake, na msipopata maji, basi tayamamuni kwa udongo safi, na mkapake nyuso zenu na mikono yenu. Hakika Allah ni Msamehevu, Mwenye kughofiri.

تَغْتَسِلُوْا ؕ وَاِنْ كُنْتُمْ مَّرْضٰٓى اَوْ عَلٰى
سَفَرٍ اَوْ جَآءَ اَحَدٌ مِّنْكُمْ مِّنَ الْغَآئِطِ اَوْ
لٰمَسْتُمُ النِّسَآءَ فَلَمْ تَجِدُوْا مَآءً فَتَيَمَّمُوْا
صَعِيْدًا طَيِّبًا فَامْسَحُوْا بِوُجُوْهِكُمْ
وَاَيْدِيْكُمْ ؕ اِنَّ اللّٰهَ كَانَ عَفُوًّا غَفُوْرًا ﴿٤٣﴾

45. Je, huwaoni wale waliopewa sehemu ya Kitabu? Wananunua upotevu na wanataka kwamba mpotee njia.

اَلَمْ تَرَ اِلَى الَّذِيْنَ اُوْتُوْا نَصِيْبًا مِّنَ
الْكِتٰبِ يَشْتَرُوْنَ الضَّلٰلَةَ وَيُرِيْدُوْنَ
اَنْ تَضِلُّوا السَّبِيْلَ ﴿٤٤﴾ؕ

46. Na Allah anawajua sana maadui zenu; na Allah Anatosha kuwa Mlinzi, na Allah Anatosha kuwa Msaidizi.

وَاللّٰهُ اَعْلَمُ بِاَعْدَآئِكُمْ ؕ وَكَفٰى بِاللّٰهِ
وَلِيًّا ۙ وَّكَفٰى بِاللّٰهِ نَصِيْرًا ﴿٤٥﴾

47. Miongoni mwa Mayahudi wamo ambao hubadilisha maneno kutoka mahali pao, na husema: Tumesikia na tumeasi: nawe sikia bila kusikilizwa; na (husema) Raa'inaa kwa kuzigeuza ndimi zao, na kuitusi dini; na kama wao wangalisema, Tumesikia na tumetii, na usikie na utuangalie, ingalikuwa bora kwao na vizuri zaidi. Lakini Allah Amewalaani kwa kufuru zao, basi hawaamini ila kidogo tu.

مِنَ الَّذِيْنَ هَادُوْا يُحَرِّفُوْنَ الْكَلِمَ عَنْ
مَّوَاضِعِهٖ وَيَقُوْلُوْنَ سَمِعْنَا وَعَصَيْنَا
وَاسْمَعْ غَيْرَ مُسْمَعٍ وَّرَاعِنَا لَيًّا
بِاَلْسِنَتِهِمْ وَطَعْنًا فِى الدِّيْنِ ؕ وَلَوْ اَنَّهُمْ
قَالُوْا سَمِعْنَا وَاَطَعْنَا وَاسْمَعْ وَانْظُرْنَا
لَكَانَ خَيْرًا لَّهُمْ وَاَقْوَمَ ۙ وَلٰكِنْ لَّعَنَهُمُ
اللّٰهُ بِكُفْرِهِمْ فَلَا يُؤْمِنُوْنَ اِلَّا قَلِيْلًا ﴿٤٦﴾

48. Enyi mliopewa Kitabu! Yaaminini Tuliyoyateremsha yenye kusadikisha

يٰٓاَيُّهَا الَّذِيْنَ اُوْتُوا الْكِتٰبَ اٰمِنُوْا بِمَا نَزَّلْنَا

yanamkumbusha mtu asili yake (sura 77:21), basi kumfanya mtu awe na unyenyekevu, udongo unamkumbusha kitu kingine dhalili alichoumbiwa, (Amewaumbeni kwa udongo, sura 30:21).

Aya 47. *Tumesikia na tumeasi;* Maana halisi ya kipande hiki cha aya haitakuwa imetolewa kwa uadilifu kwa njia ya tafsiri tu kwa sababu hapa wanafiki wanaelezwa kuwa wamevitamka vibaya kwa makusudi baadhi ya vifungu vya maneno vya kawaida ili kuvipindisha kwa nia ya kumtukana Mtukusu Mtume s.a.w. Waaminio walitumia kifungu cha maneno *'sami'naa* na *atwa'naa* chenye maana ya tumesikia na tumetiii. Badala ya usemi *atwa'naa* wanafiki walisema *'aswaynaa* (neno lililotumika katika maandiko halisi ya aya hii likimaanisha kwamba tumesikia na tumeasi. Hata hivyo walilitamka haraka haraka kwa nia ya kumpoteza msikilizaji kwamba wamesema *atwa'naa* badala ya *'aswaynaa.* Lakini msikilizaji hodari asingekosa kuujua udanganyifu huu na tusi lilioashiriwa. Tena wakalitamka neno *raainaa* kwa kupindisha ulimi nusu bi nusu baina ya *raainaa* na *raaiinaa*, *raainaa* lina maana ya utuhurumie ambapo *raaiinaa* lina maana ya ewe mchungaji wa kondoo wetu." Kwa mara nyingine tena hili lilikuwa jaribio la kumtukana Mtukufu Mtume s.a.w. chini ya kivuli cha matamshi.

مُصَدِّقًا لِّمَا مَعَكُمْ مِّنْ قَبْلِ اَنْ نَّطْمِسَ
وُجُوْهًا فَنَرُدَّهَا عَلٰٓى اَدْبَارِهَآ اَوْ
نَلْعَنَهُمْ كَمَا لَعَنَّآ اَصْحٰبَ السَّبْتِ ؕ
وَكَانَ اَمْرُ اللّٰهِ مَفْعُوْلًا ﴿٤٧﴾

yale yaliyo pamoja nanyi, kabla Hatujawaangamiza baadhi ya viongozi wenu na kuwafanya wageuze migongo yao na kutimua mbio, au Tuwalaani kama tulivyowalaani watu wa Sabato. Na amri ya Allah ndiyo yenye kutekelezwa.

اِنَّ اللّٰهَ لَا يَغْفِرُ اَنْ يُّشْرَكَ بِهٖ وَيَغْفِرُ مَا
دُوْنَ ذٰلِكَ لِمَنْ يَّشَآءُ ۚ وَمَنْ يُّشْرِكْ بِاللّٰهِ
فَقَدِ افْتَرٰٓى اِثْمًا عَظِيْمًا ﴿٤٨﴾

49. Hakika Allah Hasamehi kushirikishwa naye, na Husamehe yaliyo nyuma ya hayo kwa Amtakaye. Na anayemshirikisha Allah bila shaka amebuni dhambi kubwa.

اَلَمْ تَرَ اِلَى الَّذِيْنَ يُزَكُّوْنَ اَنْفُسَهُمْ ؕ بَلِ
اللّٰهُ يُزَكِّيْ مَنْ يَّشَآءُ وَلَا يُظْلَمُوْنَ فَتِيْلًا ﴿٤٩﴾

50. Je, huwaoni wale wajitakasao nafsi zao? Bali Allah Humtakasa Ampendaye, nao hawatadhulumiwa hata kidogo.

اُنْظُرْ كَيْفَ يَفْتَرُوْنَ عَلَى اللّٰهِ
الْكَذِبَ ؕ وَكَفٰى بِهٖٓ اِثْمًا مُّبِيْنًا ﴿٥٠﴾ ع ٨

51. Angalia jinsi wanavyotunga uwongo juu ya Allah, na hii yatosha kuwa dhambi iliyo dhahiri.

FUNGU 8

اَلَمْ تَرَ اِلَى الَّذِيْنَ اُوْتُوْا نَصِيْبًا مِّنَ
الْكِتٰبِ يُؤْمِنُوْنَ بِالْجِبْتِ وَالطَّاغُوْتِ
وَيَقُوْلُوْنَ لِلَّذِيْنَ كَفَرُوْا هٰٓؤُلَآءِ اَهْدٰى
مِنَ الَّذِيْنَ اٰمَنُوْا سَبِيْلًا ﴿٥١﴾

52. Je, huwaoni wale waliopewa sehemu ya Kitabu? Wanamwamini mchawi na shetani, na husema juu ya wale waliokufuru kuwa hao wameongoka zaidi katika njia kuliko wale walioamini.

اُولٰٓئِكَ الَّذِيْنَ لَعَنَهُمُ اللّٰهُ ؕ وَمَنْ يَّلْعَنِ
اللّٰهُ فَلَنْ تَجِدَ لَهٗ نَصِيْرًا ﴿٥٢﴾

53. Hao ndio Allah Amewalaani, na ambaye Allah Amemlaani basi hutamwona kuwa na msaidizi.

اَمْ لَهُمْ نَصِيْبٌ مِّنَ الْمُلْكِ فَاِذًا لَّا
يُؤْتُوْنَ النَّاسَ نَقِيْرًا ﴿٥٣﴾

54. Ama wanayo sehemu ya ufalme? Basi hapo wasingaliwapa watu hata kokwa.

Aya 49. *Hasamehi.* Siyo mradi wake kuwa anayeabudu masanamu hawezi kutubu au kwamba toba yake haiwezi kupokelewa hata hapa duniani, la. Bali maneno hayo yanahusu wakati wa kufa, yaani anayekufa katika hali ya shirki hatasamehewa.

55. Au wanawafanyia watu husuda kwa yale aliyowapa Allah kwa ukarimu Wake? Basi bila shaka tuliwapa watoto wa Ibrahimu Kitabu na hekima, na Tukawapa ufalme mkuu.

أَمْ يَحْسُدُونَ النَّاسَ عَلَىٰ مَآ ءَاتَىٰهُمُ اللَّهُ مِن فَضْلِهِۦ ۚ فَقَدْ ءَاتَيْنَآ ءَالَ إِبْرَٰهِيمَ ٱلْكِتَٰبَ وَٱلْحِكْمَةَ وَءَاتَيْنَٰهُم مُّلْكًا عَظِيمًا ﴿٥٥﴾

56. Basi yuko miongoni mwao anayemwamini, na yuko miongoni mwao anayejiepusha naye. Na Jahanamu yatosha kuunguza.

فَمِنْهُم مَّنْ ءَامَنَ بِهِۦ وَمِنْهُم مَّن صَدَّ عَنْهُ ۚ وَكَفَىٰ بِجَهَنَّمَ سَعِيرًا ﴿٥٦﴾

57. Hakika wale waliozikataa Aya Zetu, karibuni Tutawaingiza katika Moto; kila mara ngozi zao zitakapoungua, Tutawabadilishia ngozi badala ya zile ili waonje adhabu. Hakika Allah ni Mwenye nguvu, Mwenye hekima.

إِنَّ ٱلَّذِينَ كَفَرُوا۟ بِـَٔايَٰتِنَا سَوْفَ نُصْلِيهِمْ نَارًا كُلَّمَا نَضِجَتْ جُلُودُهُم بَدَّلْنَٰهُمْ جُلُودًا غَيْرَهَا لِيَذُوقُوا۟ ٱلْعَذَابَ ۗ إِنَّ ٱللَّهَ كَانَ عَزِيزًا حَكِيمًا ﴿٥٧﴾

58. Na wale walioamini na kufanya vitendo vizuri, karibuni Tutawaingiza katika Mabustani yapitayo mito chini yao kwa kukaa humo milele; Humo watakuwa na wenzi waliotakaswa; na Tutawaingiza katika kivuli kizito.

وَٱلَّذِينَ ءَامَنُوا۟ وَعَمِلُوا۟ ٱلصَّٰلِحَٰتِ سَنُدْخِلُهُمْ جَنَّٰتٍ تَجْرِى مِن تَحْتِهَا ٱلْأَنْهَٰرُ خَٰلِدِينَ فِيهَآ أَبَدًا ۖ لَّهُمْ فِيهَآ أَزْوَٰجٌ مُّطَهَّرَةٌ ۖ وَنُدْخِلُهُمْ ظِلًّا ظَلِيلًا ﴿٥٨﴾

59. Hakika Allah Anawaamuruni kuzirudisha amana kwa wanaozistahili, na ya kwamba mnapohukumu baina ya watu mhukumu kwa uadilifu; bila shaka mawaidha Anayowatoleeni Allah ni mazuri sana; Hakika Allah ndiye Asikiaye, Aonaye.

إِنَّ ٱللَّهَ يَأْمُرُكُمْ أَن تُؤَدُّوا۟ ٱلْأَمَٰنَٰتِ إِلَىٰٓ أَهْلِهَا وَإِذَا حَكَمْتُم بَيْنَ ٱلنَّاسِ أَن تَحْكُمُوا۟ بِٱلْعَدْلِ ۚ إِنَّ ٱللَّهَ نِعِمَّا يَعِظُكُم بِهِۦٓ ۗ إِنَّ ٱللَّهَ كَانَ سَمِيعًۢا بَصِيرًا ﴿٥٩﴾

60. Enyi mlioamini! Mtiini Allah na Mtiini Mtume Wake na wale wenye

يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُوٓا۟ أَطِيعُوا۟ ٱللَّهَ وَأَطِيعُوا۟

Aya 59. *Amana.* Yaani kazi au kitu ambacho mtu amekabidhiwa; au amri ya Mungu anayowapa watumishi Wake; au ahali za mtu (Lane). Mtume *s.a.w.* alisema ya kuwa cheo au kazi yenye mamlaka pia ni amana (Muslim sura *Imaarat*)

Aya 60. Muundo wa lugha ya Kiarabu wa fungu la maneno *'uulil amri minkum* (wenye

الرَّسُوْلَ وَاُولِى الْاَمْرِ مِنْكُمْ ۚ فَاِنْ
تَنَازَعْتُمْ فِىْ شَىْءٍ فَرُدُّوْهُ اِلَى اللّٰهِ
وَالرَّسُوْلِ اِنْ كُنْتُمْ تُؤْمِنُوْنَ بِاللّٰهِ وَالْيَوْمِ
الْاٰخِرِ ؕ ذٰلِكَ خَيْرٌ وَّاَحْسَنُ تَاْوِيْلًا ﴿٥٩﴾ ع

mamlaka juu yenu; na kama mkigombana juu ya jambo lo lote, basi lirudisheni kwa Allah na Mtume, ikiwa mnamwamini Allah na siku ya Mwisho. Hayo ni bora sana kwa matokeo.

FUNGU 9

اَلَمْ تَرَ اِلَى الَّذِيْنَ يَزْعُمُوْنَ اَنَّهُمْ اٰمَنُوْا
بِمَاۤ اُنْزِلَ اِلَيْكَ وَمَاۤ اُنْزِلَ مِنْ قَبْلِكَ
يُرِيْدُوْنَ اَنْ يَّتَحَاكَمُوْۤا اِلَى الطَّاغُوْتِ
وَقَدْ اُمِرُوْۤا اَنْ يَّكْفُرُوْا بِهٖ ؕ وَيُرِيْدُ
الشَّيْطٰنُ اَنْ يُّضِلَّهُمْ ضَلٰلًا ۢ بَعِيْدًا ﴿٦٠﴾

61. Je, huwaoni wale wanaodai ya kwamba wameamini yale yaliyoteremshwa kwako na yaliyoteremshwa kabla yako? Wanataka wakahukumiwe kwa Shetani, hali walipewa amri ya kumkataa; na Shetani anataka kuwapoteza upotevu wa mbali.

وَاِذَا قِيْلَ لَهُمْ تَعَالَوْا اِلٰى مَاۤ اَنْزَلَ اللّٰهُ
وَاِلَى الرَّسُوْلِ رَاَيْتَ الْمُنٰفِقِيْنَ
يَصُدُّوْنَ عَنْكَ صُدُوْدًا ﴿٦١﴾ ۚ

62. Na wanapoambiwa, njooni kwenye yale Aliyoyateremsha Allah, na kwa Mtume, utawaona wanafiki wanajiweka mbali nawe kabisa.

فَكَيْفَ اِذَاۤ اَصَابَتْهُمْ مُّصِيْبَةٌ ۢ بِمَا
قَدَّمَتْ اَيْدِيْهِمْ ثُمَّ جَآءُوْكَ يَحْلِفُوْنَ ۖ
بِاللّٰهِ اِنْ اَرَدْنَاۤ اِلَّاۤ اِحْسَانًا وَّتَوْفِيْقًا ﴿٦٢﴾

63. Basi inakuwaje unapowafikia msiba kwa sababu ya yale iliyoyatanguliza mikono yao kisha wanakujia wakiapa kwa jina la Allah wakisema kwamba hatukutaka ila wema na mapatano.

اُولٰٓئِكَ الَّذِيْنَ يَعْلَمُ اللّٰهُ مَا فِىْ قُلُوْبِهِمْ ۖ
فَاَعْرِضْ عَنْهُمْ وَعِظْهُمْ وَقُلْ لَّهُمْ فِىْۤ
اَنْفُسِهِمْ قَوْلًا ۢ بَلِيْغًا ﴿٦٣﴾

64. Hao ndio ambao Allah Anayajua yaliyomo mioyoni mwao, basi waache, na uwanasihi na uwaambie maneno yatakayoingia katika nafsi zao.

mamlaka juu yenu) haujaeleweka sawasawa na baadhi ya watu. Na lenye utashi maalum ni neno *minkum* ambalo kwa hakika linaundwa na viarifu viwili vilivyounganishwa pamoja yaani *min* na *kum*. *Min* maana yake ni kutoka na *kum* maana yake ni ninyi. Kwa kulitafsiri kwa mtindo wa neno kwa neno, baadhi ya mufasirina walilielewa fungu hili la maneno kuwa na maana ya kutoka miongoni mwenu. Yaani mnatakiwa kuitii ile mamlaka ambayo inabahatika kuwa imetoka miongoni mwenu, ikiwa na maana ya mamlaka ya Kiislamu peke yake. Katika mfano huu maalum hiki kiarifu *min* kinafanya kazi ya kukiunganisha tu kile kiarifu *kum* na lile neno *uulil amri* katika uhusiano wa kumiliki na tafsiri ni lazima iwe Wale wenye mamlaka juu yenu.

Katika maana iliyopanuka zaidi maneno haya yanawakusanya hata wale wasio Waislamu Sunna na Hadithi za Mtume *s.a.w.* zimeweka jambo hili wazi ya kuwa katika mambo ya kidunia Waislamu wawatii hata hao watawala wasiokuwa Waislamu, kama hawaingii kuvuruga mambo ya dini yao.

وَمَآ اَرْسَلْنَا مِنْ رَّسُوْلٍ اِلَّا لِيُطَاعَ
بِاِذْنِ اللّٰهِ ؕ وَلَوْ اَنَّهُمْ اِذْ ظَّلَمُوْٓا اَنْفُسَهُمْ
جَآءُوْكَ فَاسْتَغْفَرُوا اللّٰهَ وَاسْتَغْفَرَ
لَهُمُ الرَّسُوْلُ لَوَجَدُوا اللّٰهَ تَوَّابًا رَّحِيْمًا ﴿٦٤﴾

65. Na Hatukumtuma Mtume ye yote ila atiiwe kwa amri ya Allah; na lau wangalikujia walipojidhulumu nafsi zao wakaomba msamaha kwa Allah, na Mtume pia akawaombea msamaha, bila shaka wangemkuta Allah, Mwenye kupokea toba Mwenye rehema.

فَلَا وَرَبِّكَ لَا يُؤْمِنُوْنَ حَتّٰى يُحَكِّمُوْكَ
فِيْمَا شَجَرَ بَيْنَهُمْ ثُمَّ لَا يَجِدُوْا فِيْٓ اَنْفُسِهِمْ
حَرَجًا مِّمَّا قَضَيْتَ وَيُسَلِّمُوْا تَسْلِيْمًا ﴿٦٥﴾

66. Siyo, kwa haki ya Mola wako, wao, hawawi wenye kuamini mpaka wakufanye hakimu katika yale waliyohitilafiana kati yao, kisha wasione chuki mioyoni mwao juu ya hukumu uliyotoa, na wanyenyekee kabisa.

وَلَوْ اَنَّا كَتَبْنَا عَلَيْهِمْ اَنِ اقْتُلُوْٓا
اَنْفُسَكُمْ اَوِ اخْرُجُوْا مِنْ دِيَارِكُمْ مَّا
فَعَلُوْهُ اِلَّا قَلِيْلٌ مِّنْهُمْ ؕ وَلَوْ اَنَّهُمْ
فَعَلُوْا مَا يُوْعَظُوْنَ بِهٖ لَكَانَ خَيْرًا لَّهُمْ
وَاَشَدَّ تَثْبِيْتًا ﴿٦٦﴾

67. Na kama Tungeliwalazimisha ya kwamba ziueni nafsi zenu au tokeni katika nyumba zenu, wasingalifanya hivyo isipokuwa wachache tu katika hao, na kama wangalifanya waliyoagizwa ingalikuwa bora kwao na inayoimarisha zaidi.

وَّاِذًا لَّاٰتَيْنٰهُمْ مِّنْ لَّدُنَّآ اَجْرًا عَظِيْمًا ﴿٦٧﴾

68. Na ndipo Tungewapa malipo makubwa kutoka Kwetu.

وَّلَهَدَيْنٰهُمْ صِرَاطًا مُّسْتَقِيْمًا ﴿٦٨﴾

69. Na hakika Tungewaongoza njia iliyonyooka.

وَمَنْ يُّطِعِ اللّٰهَ وَالرَّسُوْلَ فَاُولٰٓئِكَ مَعَ
الَّذِيْنَ اَنْعَمَ اللّٰهُ عَلَيْهِمْ مِّنَ النَّبِيّٖنَ
وَالصِّدِّيْقِيْنَ وَالشُّهَدَآءِ وَالصّٰلِحِيْنَ ۚ
وَحَسُنَ اُولٰٓئِكَ رَفِيْقًا ﴿٦٩﴾

70. Na Mwenye kumtii Allah na Mtume, basi hao ni miongoni mwa wale Aliowaneemesha Allah -- Manabii na Masidiki na Mashahidi na Masalih; na hao ndio marafiki wema.

ذٰلِكَ الْفَضْلُ مِنَ اللّٰهِ ؕ وَكَفٰى بِاللّٰهِ
عَلِيْمًا ﴿٧٠﴾ ع ۩

71. Hiyo ni fadhili itokayo kwa Allah; na Allah Anatosha kuwa Mjuzi.

Aya 67. Maneno "ueni watu wenu" yaweza kueleweka vibaya. Tafsiri sahihi ingekuwa "Ueni nafsi zenu". Hii kwa hakika haina maana kwamba waliambiwa wajiue wenyewe bali ni maneno tu yaliyokuwa yakiwahimiza waue ubinafsi wao na wajitupe moja kwa moja katika radhi ya Allah.

Aya 70. Katika Aya hii madaraja manne yamewekwa kwa ajili ya Waislamu: (1) Unabii;

FUNGU 10

يٰٓاَيُّهَا الَّذِيْنَ اٰمَنُوْا خُذُوْا حِذْرَكُمْ فَانْفِرُوْا ثُبَاتٍ اَوِ انْفِرُوْا جَمِيْعًا ﴿٧١﴾

72. Enyi mlioamini shikeni hadhari yenu, kisha tokeni kundi moja moja au tokeni nyote pamoja.

وَاِنَّ مِنْكُمْ لَمَنْ لَّيُبَطِّئَنَّ ۚ فَاِنْ اَصَابَتْكُمْ مُّصِيْبَةٌ قَالَ قَدْ اَنْعَمَ اللّٰهُ عَلَيَّ اِذْ لَمْ اَكُنْ مَّعَهُمْ شَهِيْدًا ﴿٧٢﴾

73. Na bila shaka yuko katika ninyi anayekawia nyuma, na kama unawapateni msiba, husema: Hakika Allah Amenineemesha nilipokuwa sikuhudhuria pamoja nao.

وَلَئِنْ اَصَابَكُمْ فَضْلٌ مِّنَ اللّٰهِ لَيَقُوْلَنَّ كَاَنْ لَّمْ تَكُنْۢ بَيْنَكُمْ وَبَيْنَهٗ مَوَدَّةٌ يّٰلَيْتَنِيْ كُنْتُ مَعَهُمْ فَاَفُوْزَ فَوْزًا عَظِيْمًا ﴿٧٣﴾

74. Na kama ikiwafikieni fadhili kutoka kwa Allah, husema -- kana kwamba haukuwa urafiki baina yenu na baina yake -- Laiti ningalikuwa pamoja nao na ningalipata ufaulu mkuu.

فَلْيُقَاتِلْ فِيْ سَبِيْلِ اللّٰهِ الَّذِيْنَ يَشْرُوْنَ الْحَيٰوةَ الدُّنْيَا بِالْاٰخِرَةِ ۭ وَمَنْ يُّقَاتِلْ فِيْ سَبِيْلِ اللّٰهِ فَيُقْتَلْ اَوْ يَغْلِبْ فَسَوْفَ نُؤْتِيْهِ اَجْرًا عَظِيْمًا ﴿٧٤﴾

75. Basi wapigane katika njia ya Allah wale wanaouza maisha (yao) ya dunia kwa Akhera; na anayepigana katika njia ya Allah kisha akauawa au akashinda, basi hivi karibuni Tutampa ujira mkuu.

---

(2) Usidiki; (3) Ushahidi; (4) Usalihi. Neno *ma'a* lililotumiwa katika Aya hii na ambalo limetafsiriwa *miongoni mwa* ni kama lililotumiwa katika sura 4:147 kuonyesha kuwa wanafiki wanaotubu watakuwa *ma'almuminin,* yaani miongoni mwa waaminio. Ndiyo kusema nao pia watakuwa waaminio. Kadhalika katika sura 3:194 waaminio wamefundishwa kuomba hivi, "Utufishe *ma'alabraar"* yaani katika wema. Hivyo katika Aya hii neno *Ma'alladhiina an'amallaahu* maana yake ni watakuwa katika wale aliowaneemesha Allah.

Maoni haya yanakubaliwa na Abu Hayyan, mtungaji maarufu wa Kitabu Bahr-ul-Muhit, na pia Ar-Raghib. Katika Bahr-ul-Muhit (jalada 3, uk. 278) mmeandikwa maneno ya Ar-Raghib yanayosema: "Allah.- amewagawanya waaminio katika sehemu nne katika Aya hii, na amewawekea madaraja manne ambayo mengine yao ni ya chini kuliko mengine, na amewahimiza waaminio wasibaki nyuma ya madaraja haya."

Kadhalika katika Ruuh-ul-Ma'aani, ambayo ni tafsiri ijulikanayo sana, mmeandikwa maelezo ya Aya hii kwa maneno haya. "Unabii ni wa namna mbili, *wa desturi na wa maalum.* Unabii *wa maalum* yaani Utume wa kuleta sheria, sasa haupatikani; Lakini *utume wa desturi,* bado unaendelea ." Na Mtume *s.a.w.* alisema "Kama (mwanangu) Ibrahimu angeishi angekuwa Nabii" (Ibni Maja, sura ya *Janaaiz*).

Aya 73. Aya hii inawahusu wanafiki na inaonyesha tabia zao mbili: (1) Kunapokuwa vita hawaendi pamoja na Waislamu, na wanafurahi kukosa kwenda; (2) hawashirikiani na Waislamu katika huzuni na furaha zao, bali wao hujali habari zinazowahusu wao wenyewe tu.

وَمَا لَكُمْ لَا تُقَاتِلُوْنَ فِيْ سَبِيْلِ اللّٰهِ وَالْمُسْتَضْعَفِيْنَ مِنَ الرِّجَالِ وَالنِّسَآءِ وَالْوِلْدَانِ الَّذِيْنَ يَقُوْلُوْنَ رَبَّنَآ اَخْرِجْنَا مِنْ هٰذِهِ الْقَرْيَةِ الظَّالِمِ اَهْلُهَا ۚ وَاجْعَلْ لَّنَا مِنْ لَّدُنْكَ وَلِيًّا ۙ وَّاجْعَلْ لَّنَا مِنْ لَّدُنْكَ نَصِيْرًا ﴿٧٥﴾

76. Na mna nini hampigani katika njia ya Allah na ya wale walio dhaifu katika wanaume na wanawake na watoto ambao husema: Mola wetu, Ututoe katika mji huu ambao watu wake ni wadhalimu, na Utujaalie mlinzi kutoka Kwako na Utujaalie msaidizi kutoka Kwako.

اَلَّذِيْنَ اٰمَنُوْا يُقَاتِلُوْنَ فِيْ سَبِيْلِ اللّٰهِ ۚ وَالَّذِيْنَ كَفَرُوْا يُقَاتِلُوْنَ فِيْ سَبِيْلِ الطَّاغُوْتِ فَقَاتِلُوْٓا اَوْلِيَآءَ الشَّيْطٰنِ ۚ اِنَّ كَيْدَ الشَّيْطٰنِ كَانَ ضَعِيْفًا ﴿٧٦﴾ ع

77. Wale walioamini wanapigana katika njia ya Allah, lakini waliokufuru wanapigana katika njia ya Shetani, basi piganeni na marafiki wa Shetani; hakika hila za Shetani ni dhaifu.

FUNGU 11

اَلَمْ تَرَ اِلَى الَّذِيْنَ قِيْلَ لَهُمْ كُفُّوْٓا اَيْدِيَكُمْ وَاَقِيْمُوا الصَّلٰوةَ وَاٰتُوا الزَّكٰوةَ ۚ فَلَمَّا كُتِبَ عَلَيْهِمُ الْقِتَالُ اِذَا فَرِيْقٌ مِّنْهُمْ يَخْشَوْنَ النَّاسَ كَخَشْيَةِ اللّٰهِ اَوْ اَشَدَّ خَشْيَةً ۚ وَقَالُوْا رَبَّنَا لِمَ كَتَبْتَ عَلَيْنَا الْقِتَالَ ۚ لَوْلَآ اَخَّرْتَنَآ اِلٰٓى اَجَلٍ قَرِيْبٍ ۭ قُلْ مَتَاعُ الدُّنْيَا قَلِيْلٌ ۚ وَالْاٰخِرَةُ خَيْرٌ لِّمَنِ اتَّقٰى ۣ وَلَا تُظْلَمُوْنَ فَتِيْلًا ﴿٧٧﴾

78. Je! huwaoni wale walioambiwa; Izuieni mikono yenu, na simamisheni Sala, na toeni Zaka. Lakini walipolazimishwa kupigana, mara kundi moja katika wao wakawaogopa watu kama kumwogopa Mungu au kwa hofu zaidi, na wakasema: Mola wetu, mbona Umetulazimisha kupigana? Kwa nini hukutuahirisha mpaka muda ulio karibu? Sema: Starehe ya dunia ni kidogo, lakini Akhera ni bora kwa mwenye kumcha; wala hamtadhulumiwa hata kidogo.

اَيْنَ مَا تَكُوْنُوْا يُدْرِكْكُّمُ الْمَوْتُ وَلَوْ كُنْتُمْ فِيْ بُرُوْجٍ مُّشَيَّدَةٍ ۭ وَاِنْ تُصِبْهُمْ حَسَنَةٌ يَّقُوْلُوْا هٰذِهٖ مِنْ عِنْدِ اللّٰهِ ۚ وَاِنْ تُصِبْهُمْ سَيِّئَةٌ يَّقُوْلُوْا هٰذِهٖ مِنْ عِنْدِكَ ۭ قُلْ كُلٌّ مِّنْ عِنْدِ اللّٰهِ ۭ فَمَالِ هٰٓؤُلَاۗءِ الْقَوْمِ لَا يَكَادُوْنَ يَفْقَهُوْنَ حَدِيْثًا ﴿٧٨﴾

79. Po pote mlipo mauti yatawafikieni, hata kama muwe ndani ya ngome madhubuti. Na kama ukiwafikia wema wanasema: Huu umetoka kwa Allah. Na kama ukiwafikia ubaya wanasema, huu umetoka kwako. Sema: Yote yametoka kwa Allah; basi wamekuwaje watu hawa hawawezi kufahamu hadithi?

Aya 76. Aya hii ni dalili ya wazi kuwa Waislamu hawakuwa wa kwanza kuanzisha mapigano. Waislamu walipigana vita ili kujilinda tu na kuwaokoa wenzao wanyonge. (Tazama sura 2:191; na 22:40).

مَآ اَصَابَكَ مِنۡ حَسَنَةٍ فَمِنَ اللّٰهِ ۘ وَمَآ اَصَابَكَ مِنۡ سَيِّئَةٍ فَمِنۡ نَّفۡسِكَ ؕ وَاَرۡسَلۡنٰكَ لِلنَّاسِ رَسُوۡلًا ؕ وَكَفٰى بِاللّٰهِ شَهِيۡدًا ﴿۸۰﴾

80. Wema uliokufikia umetoka kwa Allah; na ubaya uliokufikia, basi umetoka nafsini mwako. Nasi Tumekupeleka kwa watu kuwa Mtume; na Allah Atosha kuwa shahidi.

مَنۡ يُّطِعِ الرَّسُوۡلَ فَقَدۡ اَطَاعَ اللّٰهَ ۚ وَمَنۡ تَوَلّٰى فَمَاۤ اَرۡسَلۡنٰكَ عَلَيۡهِمۡ حَفِيۡظًا ؕ ﴿۸۱﴾

81. Mwenye kumtii Mtume, basi amemtii Allah, na anayegeuka, basi Hatukukupeleka kuwa mlinzi juu yao.

وَيَقُوۡلُوۡنَ طَاعَةٌ ۫ فَاِذَا بَرَزُوۡا مِنۡ عِنۡدِكَ بَيَّتَ طَآئِفَةٌ مِّنۡهُمۡ غَيۡرَ الَّذِىۡ تَقُوۡلُ ؕ وَاللّٰهُ يَكۡتُبُ مَا يُبَيِّتُوۡنَ ۚ فَاَعۡرِضۡ عَنۡهُمۡ وَتَوَكَّلۡ عَلَى اللّٰهِ ؕ وَكَفٰى بِاللّٰهِ وَكِيۡلًا ﴿۸۲﴾

82. Na wanasema: Tunatii; lakini wanapotoka mbele yako kundi moja miongoni mwao linashauriana usiku kinyume cha yale usemayo. Na Allah Huyaandika wanayoshauriana usiku, basi uwaachilie mbali, na umtegemee Allah, na Allah Atosha kuwa Mlinzi.

اَفَلَا يَتَدَبَّرُوۡنَ الۡقُرۡاٰنَ ؕ وَلَوۡ كَانَ مِنۡ عِنۡدِ غَيۡرِ اللّٰهِ لَوَجَدُوۡا فِيۡهِ اخۡتِلَافًا كَثِيۡرًا ﴿۸۳﴾

83. Je, hawaitafakari Qur'an? Na kama ingalitoka kwa asiyekuwa Allah, bila shaka wangalikuta ndani yake hitilafu nyingi.

Aya 83. Maneno ya Qur'an *ikhtilaafan kathiiran,* hitilafu nyingi kwa hakika yanaashiria migongano, ikiwa na maana kwamba kama mwingine ye yote asiyekuwa Allah ndiye angelikuwa mtunzi wa Qur'an Tukufu, bila shaka yo yote watu wangelikuta migongano mingi ndani yake. Maneno yafananayo na haya kuhusiana na uumbwaji wa ulimwengu yanapatikana katika 67:4 (Al-Mulk) yakitangaza kwamba haiwezekani kukuta tofauti au migongano katika kazi ya Allah.

Hitilafu. Neno hili linaweza kuwa na maana mbili: (1) kuhitilafiana maneno ya Qur'an na mafundisho yaliyomo ndani yake; au (2) kuhitilafiana kwa bishara za Qur'an na kutimizwa kwao. Qur'an haina hitilafu katika maana zote hizi na mafundisho yake yanapatana kabisa. Watu wanaodhani kuwa kuna Aya zenye kuhitilafiana na zilizo *"naasikh"* na *"mansuukh"* ni kwa sababu hawakuifikiria Qur'an kiasi cha kutosha, kama asemavyo Allah, "Je, hawaitafakari Qur'an?" (Pia tazama sura 2:107).

Kama Kitabu kinachosemwa ni cha Mungu kiwe na habari zinazohitilafiana na kupinzana, hicho hakiwezi kuwa kitabu cha Mungu. Maana haiwezekani Mungu alete sheria inayotakiwa ifanye kazi wakati mmoja kisha ipingane.

HITILAFU ZA BIBLIA

Wasomaji wangependa kujua Vitabu vya Wakristo vikoje katika jambo hili. Hivyo, tunawaandikia kidogo. Vitabu hivyo vina hitilafu za namna ambayo, utakapoziona, saa ile ile utakata shauri ya kuwa, mbali na kusema ni ufunuo wa Mungu, haviwezi hata kusemwa kuwa viliandikwa na mtu mwenye elimu au mwenye akili. Mifano ni mingi, lakini hapa tutawaonyesheni michache ya hitilafu za Biblia:-

AGANO JIPYA NA LA KALE VINAPINZANA

(1) Yesu "akaenda, akakaa katika mji ulioitwa Nazareti; ili litimie neno lililonenwa na Manabii, Ataitwa Mnazarayo" (Matt. 2:23). Unabii uliotajwa na maneno hayo haupatikani mahali po pote katika Agano la Kale. Hivyo ikiwa Injili inasema kweli, ni wazi Agano la Kale limeharibika, na mtu mbaya mmoja au zaidi aliondoa maneno hayo. Ndiyo kusema Agano la Kale linalochezewa hivyo, maneno yake hayawezi kuwa na sifa ya Neno la Mungu: maana, ni kitabu ambacho maneno yake yanaweza kubadilishwa au kuondolewa na watu. Lakini, kama Agano la Kale ni sahihi ya kwamba toka mwanzo halikuwa na maneno hayo, basi Injili imesema uwongo, na hivyo haiwezi kuwa na sifa inayopewa kazi ya mtu mwema, sembuse ya Mungu.

HITILAFU KATIKA HABARI ZA YUDA

(2) Katika Mathayo 27:3-7 imeandikwa ya kwamba Yuda, ambaye ni mwanafunzi wa Yesu aliyepokea vipande thelathini vya fedha kwa makuhani ili apate kumkamatisha Yesu akasulubiwe, baadaye alijuta kwa uovu huo alioufanya, na akawarudishia wale makuhani fedha ile, nao wakaikataa. Lakini Yuda "akavitupa vile vipande vya fedha katika hekalu, akaondoka; akaenda, akajinyonga. Wakuu wa makuhani wakavitwaa vile vipande vya fedha. . . . . .*wakavitumia kwa kununua* konde la mfinyanzi liwe mahali pa kuzikia wageni."

Lakini maneno haya yanapinzana na maneno yaliyoandikwa mahali pengine yanayosema kwamba konde hilo halikununuliwa na makuhani, bali na Yuda mwenyewe, na ya kuwa hakujinyonga, bali alianguka kifudifudi akapasuka, matumbo yake yote yakatoka. Imeandikwa, "Katika habari za Yuda, aliyewaongoza wao waliomkamata Yesu; kwa sababu alikuwa amehesabiwa pamoja na sisi, akapata sehemu ya huduma hii. Basi mtu huyu *alinunua* konde kwa ijara ya udhalimu, akaanguka kifudifudi akapasuka, matumbo yake yote yakatoka" (Matendo 1:18).

Je, mapadre wanaweza kutuambia kuwa kitabu chenye maneno yasiyopatana hivyo kinaweza kuwa cha Mungu, tukakubali? Sisi tunajua ya kuwa ndugu zetu walioingia Ukristo walikuwa hawajapeleleza habari za vitabu hivi wanavyoambiwa kucha kutwa kuwa ni vya Mungu. Tunatumai ya kuwa wenye roho safi kati yao, sasa watafunua macho na kujitoa ndani ya janga walimotiwa hali hawana habari timilifu.

HITILAFU JUU HABARI YA WANYANG'ANYI

(3) Mattayo 27:44 na Marko 15:32, imeandikwa ya kuwa wale wanyang'anyi waliosulubiwa pamoja na Yesu, nao walimlaumu, wakamshutumu na kumfyolea Yesu. Lakini Luka 23:39- 40 anasema ya kuwa si wote wawili waliomlaumu Yesu, bali mmoja: "Na mmoja wa wale wahalifu waliotungikwa alimtukana, akasema, Je, wewe si Kristo? Jiokoe nafsi yako na sisi. Lakini yule wa pili akamjibu, akamkemea akisema, Wewe humwogopi hata Mungu, nawe u katika hukumu hiyo hiyo? Nayo ni haki kwetu kwa kuwa tunapokea malipo tuliyostahili kwa matendo yetu; bali huyu hakutenda lo lote lisilofaa."

Je, kitabu chenye maneno yanayopinzana hivi kinaweza kuwa cha Mungu? Au mapadre hawamwogopi hata Mungu kwa kusema vitabu vya namna hii vimeandikwa kwa nguvu za Roho Mtakatifu! Allah akusaidieni, ndugu zetu, mmetiwa ndani ya vurugu kubwa! Tafadhali mzinduke. Mwenye busara ni yule asiyeona haya kuachilia mbali jambo lisilofaa. Ela soma mfano mwingine unaofuata:

HABARI YA KUTAMBULIKANA YESU PIA NI HITILAFU.

(4) Mathayo 26:48, Marko 14:44, Luka 22:47-48 vinaeleza ya kuwa Yuda aliwapa Mayahudi ishara ya kuwa mtu atakayembusu ndiye Yesu, wamkamate. Lakini Yohana 18:4 kinapinza jambo hili lisemalo kuwa Yuda ndiye aliyekwenda mbusu Yesu ili ajulikane kwa Mayahudi. Hicho kinaeleza, "Yesu hali akijua yote yatakayompata, akatokea, akawaambia ni nani mnayemtafuta? Wao wakajibu ni Yesu Mnazareti. Yesu akawaambia. Ni mimi. Yuda naye aliyemsaliti alikuwa amesimama pamoja nao. Basi alipowaambia, Ni mimi, walirudi nyuma, wakaanguka chini."

Maelezo haya ya Yohana ni dhahiri yamekwenda upande. Na vitabu hivyo vinaitwa "Neno la Mungu"yaani vilifunuliwa na Mungu. Je, rafiki Mkristo, bado ungali unasadiki kuwa haya maneno yanayopingana yametoka kwa Mungu mmoja? Huu hapa mfano mwingine:

HATA MAAGIZO ALIYOTOA YESU HAYAPATANI

(5) Mathayo 10:9 na Luka 22:35vinasema kuwa Yesu alipowatuma wanafunzi wake kuhubiri, aliwaambia wasichukuwe jumla ya vitu, wala viatu, wala fimbo. Lakini Marko 6:9 kinasema, walikatazwa wasichukue kitu cha njiani isipokuwa fimbo tu, lakini wajifungie vitu pia. Na Petro mwanafunzi wa Yesu alivaa viatu (Matendo 12:8). Ni wazi hitilafu ya namna hii inaweza kuwa katika vitabu vya watu, si vya Mungu. Ndugu Mkristo, lini utaachilia mbali vitabu hivi vyenye vurugu? Tazama tena mfano mwingine:

YESU ALISULUBIWA LINI? HAWAPATANI

(6) Marko 15:25 kinasema ya kuwa ilikuwa saa tatu Yesu aliposulubiwa. Lakini Yohana 19:14 kinaeleza ya kuwa saa sita ndiyo hukumu ya kumsulubisha Yesu ilipokatwa na hakimu. Mmoja katika hawa waandishi wawili lazima maneno yake yawe si ya kweli. Ndiyo kusema kama Agano Jipya ni kitabu cha Mungu, hata hivyo kina maneno mengine yasiyokuwa ya kweli. Je, kitabu cha Mungu kinaweza kuwa hivyo? Hatumlazimishi Mkristo kuacha kusadiki vitabu hivyo kama bado anataka, lakini asikose kukumbuka ya kuwa baada ya kubainishiwa jambo hili waziwazi hivi hatokuwa na udhuru mbele ya Allah. Akiwa radhi kujidanganya mwenyewe na kujisingizia kuridhika na vitabu vya dini vyenye upungufu usiofichika kama huu, basi ni shauri lake, maana tumekwisha mwonyesha uwazi wote kwa nia safi. Tafadhali soma hii hoja nyingine.

YOHANA ALIMTAMBUAJE YESU? PIA HAWAPATANI!

(7) Yohana 1:29-34 kinaeleza ya kuwa Yohana Mbatizaji alimtambua Yesu kuwa ndiye mwana-kondoo wa Mungu, na ya kuwa hangemjua ila kwa sababu alijulishwa na (Mungu) aliyempeleka kubatiza kwa maji. Lakini Mathayo 11:2 na Luka 7:19 imeandikwa ya kwamba "Yohana aliposikia huko gerezani matendo yake Kristo, alituma wanafunzi wake kumwuliza, Wewe ndiwe yule ajaye au tumtazamie mwingine?' Habari hizi mbili ni hitilafu kabisa, na hakuna njia ya kuzipatanisha kwa uaminifu. Ah! zote mbili zimetoka kwa Mungu mmoja hizi? Ndugu Mkristo, mpaka sasa natumai umebadili mawazo yako kiasi cha kutosha. Kiri waziwazi na usimwogope mtu ila Mungu wako tu. Huna kosa hata kidogo kusadiki kuwa Agano jipya si kitabu cha Mungu. Jihadhari, mtu asikudanganye. Sasa tupande juu kwenye Agano la Kale:

TORATI ILIANDIKWA NA NANI?

(8) Inasemekana ya kuwa Torati iliandikwa na Musa, na hivyo, wanasema, lazima iwe sahihi. Je, ni kweli iliandikwa na Musa? Torati yenyewe inasema; "Basi Musa huyo Mtumishi wa Jehova alikufa huko nchi ya Moabi, kwa neno la Jehova. Akamzika bondeni katika nchi ya Moabi kuelekea Bethi-peori" (Kumbukumbu ya Torati 34:5-6). Ni wazi maneno hayo yasingeweza kuandikwa na Musa mwenyewe. Mtu mwingine aliyaandika hayo. Ni ushahidi wa wazi ya kuwa watu waliingiza maneno yao katika maneno ya Mungu wapendavyo. Hivyo ni vigumu kupambanua ni yepi maneno ya Mungu na yepi maneno ya watu katika vitabu hivyo. Kikombe cha usaha kikitiwa katika ndoo ya maziwa hunajisika maziwa yote, mtu asitake kuyanywa. Tafadhali fikiri, ndugu Mkristo.

وَاِذَا جَآءَهُمْ اَمْرٌ مِّنَ الْاَمْنِ اَوِ
الْخَوْفِ اَذَاعُوْا بِهٖ ؕ وَلَوْ رَدُّوْهُ اِلَى
الرَّسُوْلِ وَاِلٰٓى اُولِى الْاَمْرِ مِنْهُمْ
لَعَلِمَهُ الَّذِيْنَ يَسْتَنْۢبِطُوْنَهٗ مِنْهُمْ ؕ
وَلَوْ لَا فَضْلُ اللّٰهِ عَلَيْكُمْ وَرَحْمَتُهٗ
لَاتَّبَعْتُمُ الشَّيْطٰنَ اِلَّا قَلِيْلًا ﴿٨٣﴾

84. Na linapowafikia jambo lo lote la amani au la hofu hulitangaza; na kama wangalilipeleka kwa Mtume na kwa wenye mamlaka kati yao, bila shaka wangalijua wale wanaolipeleleza miongoni mwao. Na kama isingalikuwa fadhili za Allah juu yenu na rehema Zake, kwa yakini mngalimfuata Shetani isipokuwa wachache tu.

فَقَاتِلْ فِىْ سَبِيْلِ اللّٰهِ ۚ لَا تُكَلَّفُ اِلَّا
نَفْسَكَ وَحَرِّضِ الْمُؤْمِنِيْنَ ۚ عَسَى
اللّٰهُ اَنْ يَّكُفَّ بَاْسَ الَّذِيْنَ كَفَرُوْا ؕ
وَاللّٰهُ اَشَدُّ بَاْسًا وَّاَشَدُّ تَنْكِيْلًا ﴿٨٤﴾

85. Basi upigane katika njia ya Allah, hutakalifishwa ila nafsi yako, na uwahimize waaminio, huenda Allah Akazuia mashambulio ya wale waliokufuru, na Allah ndiye Mkali wa kushambulia na Mkali wa kuadhibu.

مَنْ يَّشْفَعْ شَفَاعَةً حَسَنَةً يَّكُنْ لَّهٗ نَصِيْبٌ
مِّنْهَا ۚ وَمَنْ يَّشْفَعْ شَفَاعَةً سَيِّئَةً يَّكُنْ لَّهٗ

86. Atakayeombea maombezi mema atapata sehemu katika hayo, na atakayeombea maombezi mabaya

MICHAL BINTI SAUL ALIZAA AU HAPANA?

(9) 2 Samuel 6:23 imeandikwa, "Na Michal binti Saul hakuwa na mtoto mpaka siku ya kufa kwake." Lakini hicho hicho sura 21:8 kinasema, "Lakini mfalme alichukua wana wawili wa Rizpah binti Aiah, aliomzalia Saul, Armoni na Mefibosheth; na wana watano wa Michal binti Saul." Je, inawezekana Michal aliyekufa hana mtoto, mara awe aliyekuwa na wana watano? Hili au lile moja si kweli. Neno lisilo la kweli kuwa katika "Kitabu cha Mungu" ni jambo ambalo mtu ye yote hawezi kusadiki sembuse Mkristo. Chini inafuata hoja ya kumi inayozidi kuthibitisha kuwa Biblia ina hitilafu nyingi sana ndani yake na haiwezi kuwa ni neno la Mungu.

BABA NA MWANAWE WANAWEZA KUWA NA UMRI MMOJA?

(10) Katika 2 Mambo ya Siku 21:19-20 imeandikwa ya kuwa Jehoram alipotawala alikuwa na umri wa miaka 32 na akatawala Yerusalemu kwa miaka 8 akafa mwenye umri wa miaka 42. Na hapo hapo katika 22:1-2 imeandikwa ya kwamba alipokufa huyo Jehoram watu wa Yerusalem wakamtawalisha kitinda mimba wake aitwaye Ahazia. Sasa tazama wanasema, "Alipotawala Ahazia alikuwa mwana wa miaka 42." Je, inawezekana ya kuwa baba mtu afe leo na umri wa miaka 42 na mwanawe wa mwisho kesho naye awe na umri wa miaka 42 pia? Je, baba na mwanawe wa mwisho walizaliwa siku moja? Bado mapadre wanataka tusadiki vitabu hivyo kuwa sahihi na havina ila! Tunawaomba Wakristo wajiepushe na dini za namna hii, na wasome Qur'an, waone Neno sahihi la Allah lilivyo.

Aya 86. Tafsiri hii inayafanya matumizi ya aya hii kuwa finyu kwa kuhusishwa na maamkio ya mdomo ya kutakiana mema ambapo onyo lililomo humo lina matumizi mapana zaidi. Kwa hakika linafunika siyo tu salamu za mdomo bali pia linakusudia zawadi za kila namna kujibizwa kwa zilizo bora zaidi au kwa akali kwa za kiwango kile kile.

كِفْلٌ مِّنْهَا ۗ وَكَانَ اللّٰهُ عَلٰى كُلِّ شَىْءٍ مُّقِيْتًا ﴿٨٦﴾

atapata sehemu ya matokeo mabaya ya maombezi hayo. Na Allah ni Mwenye uwezo juu ya kila kitu.

وَاِذَا حُيِّيْتُمْ بِتَحِيَّةٍ فَحَيُّوْا بِاَحْسَنَ مِنْهَآ اَوْ رُدُّوْهَا ۗ اِنَّ اللّٰهَ كَانَ عَلٰى كُلِّ شَىْءٍ حَسِيْبًا ﴿٨٧﴾

87. Na mnaposalimiwa kwa maamkio, basi itikieni kwa yaliyo bora kuliko hayo, au mrejeshe hayo hayo; hakika Allah Anafanya hesabu ya kila kitu.

اَللّٰهُ لَآ اِلٰهَ اِلَّا هُوَ ۗ لَيَجْمَعَنَّكُمْ اِلٰى يَوْمِ الْقِيٰمَةِ لَا رَيْبَ فِيْهِ ۗ وَمَنْ اَصْدَقُ مِنَ اللّٰهِ حَدِيْثًا ﴿٨٨﴾ ع

88. Allah, hakuna aabudiwaye ila Yeye tu, kwa yakini Atawakusanyeni siku ya Kiyama, haina shaka ndani yake; na nani mkweli zaidi katika maneno kuliko Allah?

FUNGU 12

فَمَا لَكُمْ فِى الْمُنٰفِقِيْنَ فِئَتَيْنِ وَاللّٰهُ اَرْكَسَهُمْ بِمَا كَسَبُوْا ۗ اَتُرِيْدُوْنَ اَنْ تَهْدُوْا مَنْ اَضَلَّ اللّٰهُ ۗ وَمَنْ يُّضْلِلِ اللّٰهُ فَلَنْ تَجِدَ لَهٗ سَبِيْلًا ﴿٨٩﴾

89. Basi imekuwaje ninyi kuwa makundi mawili katika habari ya wanafiki, na hali Allah Amewageuza kwa sababu ya yale waliyoyachuma? Je, mnataka kumwongoza ambaye Allah Amemhukumu kupotea? Na Aliyemhukumu Allah kwamba amekwisha potea, basi kwa ajili yake hutapata njia.

وَدُّوْا لَوْ تَكْفُرُوْنَ كَمَا كَفَرُوْا فَتَكُوْنُوْنَ سَوَآءً فَلَا تَتَّخِذُوْا مِنْهُمْ اَوْلِيَآءَ حَتّٰى يُهَاجِرُوْا فِىْ سَبِيْلِ اللّٰهِ ۗ فَاِنْ تَوَلَّوْا فَخُذُوْهُمْ وَاقْتُلُوْهُمْ حَيْثُ وَجَدْتُّمُوْهُمْ ۠ وَلَا تَتَّخِذُوْا مِنْهُمْ وَلِيًّا وَّلَا نَصِيْرًا ﴿٩٠﴾

90. Wanataka lau mngekufuru kama walivyokufuru wao ili muwe sawa sawa. Basi msiwafanye baadhi yao kuwa marafiki mpaka wahame katika njia ya Allah; na kama wakikenge-uka, basi wakamateni na wauweni po pote mnapowapata; wala msifanye rafiki katika wao wala msaidizi.

Aya 87. Maamkio ya Kiislamu ni *Assalaamu 'alaikum* (amani ya Allah iwe juu yenu), na pengine yanazidishwa maneno, *warahmatullaahi wa barakaatuhuu* (na rehema za Allah na baraka Zake) ili kufuata amri hii isemayo "Itikieni kwa yaliyo bora," "au mrejeshe hayo hayo." Maana yake ni kuwa kama mtu hawezi kuitikia kwa maamkio bora zaidi, basi aitikie kwa yale yale aliyoamkiwa yeye.

91. Isipokuwa wale wanaopatana na watu ambao mna ahadi baina yenu na wao, au wajao kwenu na vifua vyao vinaona dhiki kupigana nanyi au kupigana na watu wao; na kama Allah Angalipenda Angewapa ushindi juu yenu, ndipo wangalipigana nanyi. Na kama wakijitenga nanyi, na wasipigane nanyi, na kuwaleteeni amani, basi Allah Hakuwafanyieni njia juu yao.

إِلَّا الَّذِيْنَ يَصِلُوْنَ إِلٰى قَوْمٍ بَيْنَكُمْ
وَبَيْنَهُمْ مِّيْثَاقٌ أَوْ جَآءُوْكُمْ حَصِرَتْ
صُدُوْرُهُمْ أَنْ يُّقَاتِلُوْكُمْ أَوْ يُقَاتِلُوْا
قَوْمَهُمْ ؕ وَلَوْ شَآءَ اللّٰهُ لَسَلَّطَهُمْ
عَلَيْكُمْ فَلَقٰتَلُوْكُمْ ۚ فَإِنِ اعْتَزَلُوْكُمْ
فَلَمْ يُقَاتِلُوْكُمْ وَأَلْقَوْا إِلَيْكُمُ السَّلَمَ ۙ
فَمَا جَعَلَ اللّٰهُ لَكُمْ عَلَيْهِمْ سَبِيْلًا ﴿٩١﴾

92. Hivi karibuni mtawakuta wengine wanaotaka amani kwenu na amani kwa watu wao; kila wakirudishwa kwenye fitina, huangushwa humo kifudifudi, lakini kama hawajitengi nanyi na kuwaleteeni amani wala kuzuia mikono yao, basi wakamateni na kuwaua po pote mnapowapata. Na hao ndio ambao Tumekupeni juu yao dalili iliyo wazi.

سَتَجِدُوْنَ آخَرِيْنَ يُرِيْدُوْنَ أَنْ
يَّأْمَنُوْكُمْ وَيَأْمَنُوْا قَوْمَهُمْ ؕ كُلَّمَا رُدُّوْٓا
إِلَى الْفِتْنَةِ أُرْكِسُوْا فِيْهَا ۚ فَإِنْ لَّمْ
يَعْتَزِلُوْكُمْ وَيُلْقُوْٓا إِلَيْكُمُ السَّلَمَ
وَيَكُفُّوْٓا أَيْدِيَهُمْ فَخُذُوْهُمْ وَاقْتُلُوْهُمْ
حَيْثُ ثَقِفْتُمُوْهُمْ ؕ وَأُولٰٓئِكُمْ جَعَلْنَا
لَكُمْ عَلَيْهِمْ سُلْطٰنًا مُّبِيْنًا ﴿٩٢﴾ ع ۲

FUNGU 13

93. Na haimpasi mumini kumwua mumini ila kwa bahati mbaya. Na mwenye kumwua mumini kwa bahati mbaya, basi ampe uungwana mtumwa aliyeamini, na pia atoe malipo kwa warithi wake, isipokuwa waache wenyewe kuwa sadaka; lakini (aliyeuawa) akiwa ni mmoja wa watu walio ni adui zenu, hali mumini, basi ampe uungwana mtumwa aliyeamini; na kama (aliyeuawa) ni mmoja wa watu ambao mnayo ahadi baina yenu na baina yao, basi warithi wake wapewe malipo na pia apewe uungwana mtumwa aliyeamini; lakini ambaye hatampata mtumwa, basi afunge saumu miezi

وَمَا كَانَ لِمُؤْمِنٍ أَنْ يَّقْتُلَ مُؤْمِنًا إِلَّا
خَطَأً ۚ وَمَنْ قَتَلَ مُؤْمِنًا خَطَأً فَتَحْرِيْرُ
رَقَبَةٍ مُّؤْمِنَةٍ وَّدِيَةٌ مُّسَلَّمَةٌ إِلٰٓى أَهْلِهٖٓ
إِلَّآ أَنْ يَّصَّدَّقُوْا ؕ فَإِنْ كَانَ مِنْ قَوْمٍ
عَدُوٍّ لَّكُمْ وَهُوَ مُؤْمِنٌ فَتَحْرِيْرُ رَقَبَةٍ
مُّؤْمِنَةٍ ؕ وَإِنْ كَانَ مِنْ قَوْمٍ بَيْنَكُمْ
وَبَيْنَهُمْ مِّيْثَاقٌ فَدِيَةٌ مُّسَلَّمَةٌ إِلٰٓى أَهْلِهٖ
وَتَحْرِيْرُ رَقَبَةٍ مُّؤْمِنَةٍ ۚ فَمَنْ لَّمْ يَجِدْ
فَصِيَامُ شَهْرَيْنِ مُتَتَابِعَيْنِ ۙ تَوْبَةً مِّنَ

اللّٰهِ ؕ وَكَانَ اللّٰهُ عَلِيْمًا حَكِيْمًا ﴿٩٣﴾

miwili inayofuatana, ndio toba iliyoelekezwa na Allah, na Allah ni Mjuzi, Mwenye hekima.

وَمَنْ يَّقْتُلْ مُؤْمِنًا مُّتَعَمِّدًا فَجَزَآؤُهٗ جَهَنَّمُ خٰلِدًا فِيْهَا وَغَضِبَ اللّٰهُ عَلَيْهِ وَلَعَنَهٗ وَاَعَدَّ لَهٗ عَذَابًا عَظِيْمًا ﴿٩٤﴾

94. Na mwenye kumwua mumini kwa kukusudia, basi malipo yake ni Jahanam, humo atakaa, na Allah Atamghadhibikia na Atamlaani na Amemwandalia adhabu kubwa.

يٰۤاَيُّهَا الَّذِيْنَ اٰمَنُوْۤا اِذَا ضَرَبْتُمْ فِىْ سَبِيْلِ اللّٰهِ فَتَبَيَّنُوْا وَلَا تَقُوْلُوْا لِمَنْ اَلْقٰۤى اِلَيْكُمُ السَّلٰمَ لَسْتَ مُؤْمِنًا ۚ تَبْتَغُوْنَ عَرَضَ الْحَيٰوةِ الدُّنْيَا ۫ فَعِنْدَ اللّٰهِ مَغَانِمُ كَثِيْرَةٌ ؕ كَذٰلِكَ كُنْتُمْ مِّنْ قَبْلُ فَمَنَّ اللّٰهُ عَلَيْكُمْ فَتَبَيَّنُوْا ؕ اِنَّ اللّٰهَ كَانَ بِمَا تَعْمَلُوْنَ خَبِيْرًا ﴿٩٥﴾

95. Enyi mlioamini, mtakaposafiri katika njia ya Allah, basi pelelezeni sawasawa, wala msimwambie yule anayewatoleeni salamu (ya kwamba) wewe si mumini; mnataka mafao ya dunia hii, hali Allah Anayo mali nyingi. Hivi ndivyo mlikuwa zamani, lakini Allah Amewafanyieni hisani, basi chungueni sawasawa; hakika Allah Anazo habari za mnayoyatenda.

لَا يَسْتَوِى الْقٰعِدُوْنَ مِنَ الْمُؤْمِنِيْنَ غَيْرُ اُولِى الضَّرَرِ وَالْمُجٰهِدُوْنَ فِىْ سَبِيْلِ اللّٰهِ بِاَمْوَالِهِمْ وَاَنْفُسِهِمْ ؕ فَضَّلَ اللّٰهُ الْمُجٰهِدِيْنَ بِاَمْوَالِهِمْ وَاَنْفُسِهِمْ عَلَى الْقٰعِدِيْنَ دَرَجَةً ؕ وَكُلًّا وَّعَدَ اللّٰهُ الْحُسْنٰى ؕ وَفَضَّلَ اللّٰهُ الْمُجٰهِدِيْنَ عَلَى الْقٰعِدِيْنَ اَجْرًا عَظِيْمًا ﴿٩٦﴾

96. Hawawi sawa wale waaminio wakaao, isipokuwa wenye ulemavu, , na wale wafanyao juhudi katika njia ya Allah kwa mali zao na kwa nafsi zao. Allah Amewafadhili katika cheo wale wafanyao juhudi katika njia ya Allah kwa mali zao na kwa nafsi zao kuliko wakaao. Na Allah Amewaahidi wote (kupata) wema, lakini Allah Amewafadhili wale wafanyao juhudi kuliko wakaao kwa ujira mkuu,

Aya 95. Maana inayojulikana katika Aya hii ni kuwa watu watakapotoa amani au kuonyesha maelekeo ya amani kwa Waislamu, basi Waislamu nao wakubali.

دَرَجٰتٍ مِّنْهُ وَمَغْفِرَةً وَّرَحْمَةً ؕ وَكَانَ اللّٰهُ
غَفُوْرًا رَّحِيْمًا ﴿٩٦﴾ ع ١٣

97. (Watapata) vyeo vitokavyo Kwake, na msamaha na rehema. Na Allah ni Msamehevu, Mrehemevu.

FUNGU 14

اِنَّ الَّذِيْنَ تَوَفّٰىهُمُ الْمَلٰٓئِكَةُ ظَالِمِيْٓ
اَنْفُسِهِمْ قَالُوْا فِيْمَ كُنْتُمْ ؕ قَالُوْا كُنَّا
مُسْتَضْعَفِيْنَ فِي الْاَرْضِ ؕ قَالُوْٓا اَلَمْ
تَكُنْ اَرْضُ اللّٰهِ وَاسِعَةً فَتُهَاجِرُوْا فِيْهَا ؕ
فَاُولٰٓئِكَ مَاْوٰىهُمْ جَهَنَّمُ ؕ وَسَآءَتْ
مَصِيْرًا ﴿٩٨﴾

98. Kwa hakika wale ambao Malaika wamewafisha hali wamedhulumu nafsi zao, (Malaika) watasema: Mlikuwa katika hali gani? Watasema: Tulikuwa tukifahamiwa wadhaifu katika ardhi. (Malaika) watasema: Je, ardhi ya Allah haikuwa na wasaa wa ninyi kuhamia humo? Basi hao ndio makao yao ni Jahanamu, nayo ni marudio mabaya;

اِلَّا الْمُسْتَضْعَفِيْنَ مِنَ الرِّجَالِ وَ النِّسَآءِ
وَالْوِلْدَانِ لَا يَسْتَطِيْعُوْنَ حِيْلَةً وَّلَا
يَهْتَدُوْنَ سَبِيْلًا ﴿٩٩﴾

99. Isipokuwa wadhaifu katika wanaume na wanawake na watoto wasio na uwezo wa hali yo yote wala hawaoni njia (ya kuokoka).

فَاُولٰٓئِكَ عَسَى اللّٰهُ اَنْ يَّعْفُوَ عَنْهُمْ ؕ
وَكَانَ اللّٰهُ عَفُوًّا غَفُوْرًا ﴿١٠٠﴾

100. Basi hao ndio huenda Allah Atawasamehe; na Allah ni Msamehevu, Mwenye kughofiri.

وَمَنْ يُّهَاجِرْ فِيْ سَبِيْلِ اللّٰهِ يَجِدْ فِي الْاَرْضِ
مُرٰغَمًا كَثِيْرًا وَّسَعَةً ؕ وَمَنْ يَّخْرُجْ مِنْۢ
بَيْتِهٖ مُهَاجِرًا اِلَى اللّٰهِ وَرَسُوْلِهٖ ثُمَّ
يُدْرِكْهُ الْمَوْتُ فَقَدْ وَقَعَ اَجْرُهٗ عَلَى اللّٰهِ ؕ
وَكَانَ اللّٰهُ غَفُوْرًا رَّحِيْمًا ﴿١٠٠﴾ ع ١٤

101. Na mwenye kuhama katika njia ya Allah, atapata mahali pengi ardhini pa kukimbilia na wasaa; na anayetoka katika nyumba yake ili kuhama kwa ajili ya Allah na Mtume Wake, kisha yakamfikia mauti, basi umehakiki ujira wake juu ya Allah; na Allah ndiye Msamehevu, Mrehemevu.

Aya 101. Hapa waaminio wanaambiwa ya kuwa hakuna udhuru kwa ajili yao kukaa majumbani hali wamezungukwa na maadui, maana wakihama kwa nia safi kwa ajili ya Allah watapata mahali pengine pa kukimbilia na wasaa mwingi.

Maneno ya Kiarabu *fii sabiilillahi* yanamaanisha kwa ajili ya Allah.

FUNGU 15

وَاِذَا ضَرَبْتُمْ فِي الْاَرْضِ فَلَيْسَ
عَلَيْكُمْ جُنَاحٌ اَنْ تَقْصُرُوْا مِنَ الصَّلٰوةِ ۖ
اِنْ خِفْتُمْ اَنْ يَّفْتِنَكُمُ الَّذِيْنَ كَفَرُوْا ؕ
اِنَّ الْكٰفِرِيْنَ كَانُوْا لَكُمْ عَدُوًّا مُّبِيْنًا ﴿١٠١﴾

102. Na mnaposafiri katika ardhi, basi si dhambi kwenu kufupisha Sala, kama mkiogopa ya kwamba wale waliokufuru watawataabisheni. Bila shaka makafiri ni adui zenu dhahiri.

وَاِذَا كُنْتَ فِيْهِمْ فَاَقَمْتَ لَهُمُ الصَّلٰوةَ
فَلْتَقُمْ طَآئِفَةٌ مِّنْهُمْ مَّعَكَ وَلْيَاْخُذُوْٓا
اَسْلِحَتَهُمْ ۫ فَاِذَا سَجَدُوْا فَلْيَكُوْنُوْا مِنْ
وَّرَآئِكُمْ ۪ وَلْتَاْتِ طَآئِفَةٌ اُخْرٰى لَمْ
يُصَلُّوْا فَلْيُصَلُّوْا مَعَكَ وَلْيَاْخُذُوْا
حِذْرَهُمْ وَاَسْلِحَتَهُمْ ۚ وَدَّ الَّذِيْنَ كَفَرُوْا
لَوْ تَغْفُلُوْنَ عَنْ اَسْلِحَتِكُمْ وَاَمْتِعَتِكُمْ
فَيَمِيْلُوْنَ عَلَيْكُمْ مَّيْلَةً وَّاحِدَةً ؕ وَلَا
جُنَاحَ عَلَيْكُمْ اِنْ كَانَ بِكُمْ اَذًى مِّنْ
مَّطَرٍ اَوْ كُنْتُمْ مَّرْضٰٓى اَنْ تَضَعُوْٓا
اَسْلِحَتَكُمْ ۚ وَخُذُوْا حِذْرَكُمْ ؕ اِنَّ اللّٰهَ
اَعَدَّ لِلْكٰفِرِيْنَ عَذَابًا مُّهِيْنًا ﴿١٠٢﴾

103. Na unapokuwa pamoja nao ukawasalisha, basi kundi moja miongoni mwao wasimame pamoja nawe na washike silaha zao; na watakapomaliza sujuda yao (rakaa moja), basi waende nyuma yenu (kwa kulinda), na lije kundi jingine ambalo halijasali, kisha wasali pamoja nawe, nao washike hadhari yao na silaha zao, (maana) wale waliokufuru wanataka mghafilike na silaha zenu na vifao vyenu ili wawavamieni mvamio wa ghafla. Wala si dhambi kwenu, ikiwa mnaona udhia kwa sababu ya mvua au mkiwa wagonjwa, kuondoa silaha zenu. Na mshike hadhari yenu; hakika Allah Amewaandalia makafiri adhabu ifedheheshayo.

فَاِذَا قَضَيْتُمُ الصَّلٰوةَ فَاذْكُرُوا اللّٰهَ قِيٰمًا
وَّقُعُوْدًا وَّعَلٰى جُنُوْبِكُمْ ۚ فَاِذَا
اطْمَاْنَنْتُمْ فَاَقِيْمُوا الصَّلٰوةَ ۚ اِنَّ الصَّلٰوةَ
كَانَتْ عَلَى الْمُؤْمِنِيْنَ كِتٰبًا مَّوْقُوْتًا ﴿١٠٣﴾

104. Basi mwishapo kusali mkumbukeni Allah kila msimamapo na mkaapo na (mlalapo) kibavu; na mtakapopata amani, basi mkasimamishe Sala. Kwa hakika Sala kwa waaminio ni faradhi iliyowekewa nyakati.

Aya 102. *Mkifupisha Sala.* Maneno haya hayasemi kuwa rakaa za Sala zipunguzwe ambazo ni mbili zilizokwisha wekwa tokeapo kwa ajili ya Sala ya safari, bali hapa inafundishwa kuharakisha Sala inapokuwa hatari ya kushambuliwa na maadui. Tafsiri hii imetolewa na Ibni Kathir na kukubaliwa na Mujahid na Dhahhak na wanazuoni wengine.

Aya 103. Katika aya hii imeelezwa njia ya kusali Sala ya jamaa wakati wa hatari. Ziko njia 11 zilizofuatwa kwa kusali Sala ya wakati wa hatari. Tazama Al-Bahrul-Muhit.

Aya 104. Mtume Muhammad *s.a.w.* ndiye anayeambiwa hapa, na kadhalika kila Mwislamu anatakiwa kushika maagizo ya Aya hii.

وَلَا تَهِنُوْا فِي ابْتِغَآءِ الْقَوْمِ ؕ اِنْ تَكُوْنُوْا
تَاْلَمُوْنَ فَاِنَّهُمْ يَاْلَمُوْنَ كَمَا تَاْلَمُوْنَ ۚ
وَتَرْجُوْنَ مِنَ اللّٰهِ مَا لَا يَرْجُوْنَ ؕ وَكَانَ
اللّٰهُ عَلِيْمًا حَكِيْمًا ﴿١٠٤﴾ ع ١٥ ١٢

105. Na msifanye uvivu kuwafuatia watu (walio maadui); kama mkipata maumivu basi wao pia wanapata maumivu kama mwumiavyo, na mnatumai kwa Allah wasiyoyatumai; na Allah ndiye Mjuzi, Mwenye hekima.

FUNGU 16

اِنَّآ اَنْزَلْنَآ اِلَيْكَ الْكِتٰبَ بِالْحَقِّ لِتَحْكُمَ
بَيْنَ النَّاسِ بِمَآ اَرٰىكَ اللّٰهُ ؕ وَلَا تَكُنْ
لِّلْخَآئِنِيْنَ خَصِيْمًا ﴿١٠٥﴾

106. Hakika Tumekuteremshia Kitabu kwa haki ili upate kuhukumu baina ya watu kama Alivyokufahamisha Allah; na wala usiwe mtetezi wa wafanyao hiyana.

وَّاسْتَغْفِرِ اللّٰهَ ؕ اِنَّ اللّٰهَ كَانَ غَفُوْرًا
رَّحِيْمًا ﴿١٠٦﴾ ۚ

107. Na umwombe Allah ghofira; bila shaka Allah ni Msamehevu, Mrehemevu.

وَلَا تُجَادِلْ عَنِ الَّذِيْنَ يَخْتَانُوْنَ اَنْفُسَهُمْ ؕ
اِنَّ اللّٰهَ لَا يُحِبُّ مَنْ كَانَ خَوَّانًا اَثِيْمًا ﴿١٠٧﴾

108. Wala usiwatetee wale wanaojihini nafsi zao; bila shaka Allah hampendi aliye haini, mwenye dhambi.

يَّسْتَخْفُوْنَ مِنَ النَّاسِ وَلَا يَسْتَخْفُوْنَ
مِنَ اللّٰهِ وَهُوَ مَعَهُمْ اِذْ يُبَيِّتُوْنَ مَا لَا
يَرْضٰى مِنَ الْقَوْلِ ؕ وَكَانَ اللّٰهُ بِمَا
يَعْمَلُوْنَ مُحِيْطًا ﴿١٠٨﴾

109. Wanajificha na watu, lakini ha-wawezi kujificha na Allah, naye Yu pamoja nao wanaposhauriana usiku kwa kauli Asiyoipenda; na Allah ni Mwenye kuyazunguka wanayoyatenda.

هٰۤاَنْتُمْ هٰٓؤُلَآءِ جٰدَلْتُمْ عَنْهُمْ فِي الْحَيٰوةِ
الدُّنْيَا ۣ فَمَنْ يُّجَادِلُ اللّٰهَ عَنْهُمْ يَوْمَ
الْقِيٰمَةِ اَمْ مَّنْ يَّكُوْنُ عَلَيْهِمْ وَكِيْلًا ﴿١٠٩﴾

110. Angalieni! ninyi mwawatetea katika maisha ya dunia, basi ni nani atakayemjadili Allah siku ya Kiyama kwa ajili yao, au ni nani atakayekuwa mlinzi juu yao?

وَمَنْ يَّعْمَلْ سُوْٓءًا اَوْ يَظْلِمْ نَفْسَهٗ ثُمَّ
يَسْتَغْفِرِ اللّٰهَ يَجِدِ اللّٰهَ غَفُوْرًا رَّحِيْمًا ﴿١١٠﴾

111. Na mwenye kutenda uovu au kujidhulumu nafsi yake, kisha akaomba ghofira kwa Allah, atamkuta Allah ni Mwenye kughofiri, Mwenye kurehemu.

وَمَنْ يَّكْسِبْ اِثْمًا فَاِنَّمَا يَكْسِبُهٗ عَلٰى نَفْسِهٖ ؕ وَكَانَ اللّٰهُ عَلِيْمًا حَكِيْمًا ﴿۱۱۲﴾

112. Na mwenye kufanya dhambi, basi huifanyia nafsi yake tu; na Allah ndiye Ajuaye, Mwenye hekima.

وَمَنْ يَّكْسِبْ خَطِيْٓـئَةً اَوْ اِثْمًا ثُمَّ يَرْمِ بِهٖ بَرِيْٓـئًا فَقَدِ احْتَمَلَ بُهْتَانًا وَّاِثْمًا مُّبِيْنًا ﴿۱۱۳﴾ ع ۱۶/۱۳

113. Na mwenye kufanya hatia au dhambi, kisha akamsingizia nayo asiye na hatia, basi kwa hakika amebeba masingizio na dhambi iliyo wazi.

FUNGU 17

وَلَوْلَا فَضْلُ اللّٰهِ عَلَيْكَ وَرَحْمَتُهٗ لَهَمَّتْ طَّآئِفَةٌ مِّنْهُمْ اَنْ يُّضِلُّوْكَ ؕ وَمَا يُضِلُّوْنَ اِلَّآ اَنْفُسَهُمْ وَمَا يَضُرُّوْنَكَ مِنْ شَيْءٍ ؕ وَاَنْزَلَ اللّٰهُ عَلَيْكَ الْكِتٰبَ وَالْحِكْمَةَ وَعَلَّمَكَ مَا لَمْ تَكُنْ تَعْلَمُ ؕ وَكَانَ فَضْلُ اللّٰهِ عَلَيْكَ عَظِيْمًا ﴿۱۱۴﴾ ع

114. Na kama isingekuwa juu yako fadhili za Allah na rehema Zake kundi moja katika hao lingekusudia kukupoteza, lakini Yeye aliivunja mipango yao. Lakini hawapotezi ila nafsi zao wala hawataweza kukudhuru chochote. Na Allah Amekuteremshia Kitabu na hekima, na Amekufundisha yale uliyokuwa huyajui; na fadhili za Allah zilizo juu yako ni kubwa.

لَا خَيْرَ فِيْ كَثِيْرٍ مِّنْ نَّجْوٰىهُمْ اِلَّا مَنْ اَمَرَ بِصَدَقَةٍ اَوْ مَعْرُوْفٍ اَوْ اِصْلَاحٍ بَيْنَ النَّاسِ ؕ وَمَنْ يَّفْعَلْ ذٰلِكَ ابْتِغَآءَ مَرْضَاتِ اللّٰهِ فَسَوْفَ نُؤْتِيْهِ اَجْرًا عَظِيْمًا ﴿۱۱۵﴾

115. Hakuna heri katika mengi wanayoshauriana kwa siri, isipokuwa (mashauri ya) yule anayeamuru kutoa sadaka au kufanya wema au kupatanisha baina ya watu; na afanyaye hiyo kwa kutaka radhi ya Allah, basi hivi karibuni Tutampa ujira mkubwa.

Aya 113. *Khatiiah,* "Hatia" ni kosa linalofanywa ama kwa kukusudia au bila kukusudia na linamhusu mwenyewe aliyelifanya. Na *Ithmun* "dhambi" ni kosa linalofanywa makusudi na linaweza kuenea kwa watu wengine pia. (Aqrab, Mufradat na Lane).

Aya 115. Aya hii inafundisha kuwa mikutano ya namna tatu ndiyo inayoleta manufaa: (1) *Kutoa sadaka*, yaani mikutano inayofanywa kwa makusudi ya kuendesha mbele hali njema za

وَمَنْ يُّشَاقِقِ الرَّسُوْلَ مِنْۢ بَعْدِ مَا تَبَيَّنَ لَهُ الْهُدٰى وَيَتَّبِعْ غَيْرَ سَبِيْلِ الْمُؤْمِنِيْنَ نُوَلِّهٖ مَا تَوَلّٰى وَنُصْلِهٖ جَهَنَّمَ ؕ وَسَآءَتْ مَصِيْرًا ﴿۱۱۶﴾ ع ۱۷ ۱۴

116. Lakini atakayemwasi Mtume baada ya kumdhihirikia mwongozo, na kufuata njia isiyo ya waaminio, Tutamgeuza alikogeukia mwenyewe na Tutamwingiza katika Jahanamu; nayo ni mahali pabaya pa kurudia.

FUNGU 18

اِنَّ اللّٰهَ لَا يَغْفِرُ اَنْ يُّشْرَكَ بِهٖ وَيَغْفِرُ مَا دُوْنَ ذٰلِكَ لِمَنْ يَّشَآءُ ؕ وَمَنْ يُّشْرِكْ بِاللّٰهِ فَقَدْ ضَلَّ ضَلٰلًۢا بَعِيْدًا ﴿۱۱۶﴾

117. Hakika Allah Hasamehi (dhambi ya) kushirikishwa na cho chote, na husamehe yaliyo minghairi ya hayo kwa Amtakaye; na anayemshirikisha Allah, basi bila shaka yeye amekwisha potea upotevu wa mbali

اِنْ يَّدْعُوْنَ مِنْ دُوْنِهٖۤ اِلَّاۤ اِنٰثًا ۚ وَاِنْ يَّدْعُوْنَ اِلَّا شَيْطٰنًا مَّرِيْدًا ﴿۱۱۷﴾

118. Hawaombi badala Yake ila masanamu, ambapo kwa hakika hawamwombi ila Shetani mwasi.

لَّعَنَهُ اللّٰهُ ۘ وَقَالَ لَاَتَّخِذَنَّ مِنْ عِبَادِكَ نَصِيْبًا مَّفْرُوْضًا ﴿۱۱۸﴾

119. (Ambaye) Allah Amemlaani; naye (Shetani) akasema: Kwa yakini nitashika sehemu maalum katika watumishi Wako

وَّلَاُضِلَّنَّهُمْ وَلَاُمَنِّيَنَّهُمْ وَلَاٰمُرَنَّهُمْ فَلَيُبَتِّكُنَّ اٰذَانَ الْاَنْعَامِ وَلَاٰمُرَنَّهُمْ فَلَيُغَيِّرُنَّ خَلْقَ اللّٰهِ ؕ وَمَنْ يَّتَّخِذِ الشَّيْطٰنَ وَلِيًّا مِّنْ دُوْنِ اللّٰهِ فَقَدْ خَسِرَ خُسْرَانًا مُّبِيْنًا ؕ ﴿۱۱۹﴾

120. Na bila shaka nitawapoteza na kuwatamanisha na kuwaamrisha basi bila shaka watayajeruhi masikio ya wanyama na ni lazima nitawaamuru basi wao bila shaka wataubadili uumbaji wa Allah. Na mwenye kumshika Shetani kuwa rafiki badala ya Allah, basi yeye amepata hasara iliyo dhahiri.

يَعِدُهُمْ وَيُمَنِّيْهِمْ ؕ وَمَا يَعِدُهُمُ الشَّيْطٰنُ اِلَّا غُرُوْرًا ﴿۱۲۰﴾

121. (Shetani) anawaahidi na kuwatamanisha; lakini Shetani hawaahidi ila udanganyifu.

maskini na wahitaji. (2) *Kufanya wema,* yaani mikutano inayofanywa kwa makusudi ya kuendesha mbele na kueneza na kutangaza au kuvumbua na kuchungua mambo ya elimu, sanaa n.k.w. (3) *Kupatanisha baina ya watu,* yaani mikutano inayokusudiwa kuamua magomvi na kuondoa mambo yanayoleta magomvi, ikiwa katika maisha ya nyumbani, au katika taifa au utawala, au kati ya mataifa. Hili linahusu vyama vyenye makusudi ya kuongoza mambo ya utawala wa taifa au nchi, kwani kusudi lao ni kukuza amani kati ya watu.

122. Hao mahali pao ni Jahanamu, wala hawatapata kimbilio kutoka humo.

أُولٰٓئِكَ مَاْوٰىهُمْ جَهَنَّمُ ۖ وَلَا يَجِدُوْنَ عَنْهَا مَحِيْصًا ﴿١٢١﴾

123. Na wale walioamini na kufanya vitendo vizuri, bila shaka hivi karibuni Tutawaingiza katika Mabustani yapitayo mito ndani yake, watakaa humo milele, ni ahadi ya Allah iliyo kweli; na nani mkweli zaidi kwa usemi kuliko Allah.

وَالَّذِيْنَ اٰمَنُوْا وَعَمِلُوا الصّٰلِحٰتِ سَنُدْخِلُهُمْ جَنّٰتٍ تَجْرِيْ مِنْ تَحْتِهَا الْاَنْهٰرُ خٰلِدِيْنَ فِيْهَآ اَبَدًا ۭ وَعْدَ اللّٰهِ حَقًّا ۭ وَمَنْ اَصْدَقُ مِنَ اللّٰهِ قِيْلًا ﴿١٢٢﴾

124. Uamuzi hautakuwa sawa na matamanio yenu, wala sawa na matamanio ya watu wa Kitabu; atakayefanya ubaya atapewa ujira wake, wala hatapata mlinzi wala msaidizi kwa ajili yake badala ya Allah.

لَيْسَ بِاَمَانِيِّكُمْ وَلَآ اَمَانِيِّ اَهْلِ الْكِتٰبِ ۭ مَنْ يَّعْمَلْ سُوْۗءًا يُّجْزَ بِهٖ ۙ وَلَا يَجِدْ لَهٗ مِنْ دُوْنِ اللّٰهِ وَلِيًّا وَّلَا نَصِيْرًا ﴿١٢٣﴾

125. Na atakayefanya vitendo vizuri, akiwa mwanamume au mwanamke, hali yeye ni mwenye kuamini - basi hao wataingia Peponi, wala hawatadhulumiwa hata kidogo.

وَمَنْ يَّعْمَلْ مِنَ الصّٰلِحٰتِ مِنْ ذَكَرٍ اَوْ اُنْثٰى وَهُوَ مُؤْمِنٌ فَاُولٰۗىِٕكَ يَدْخُلُوْنَ الْجَنَّةَ وَلَا يُظْلَمُوْنَ نَقِيْرًا ﴿١٢٤﴾

126. Na nani aliye mbora kwa dini kuliko yule ambaye amejitupa dhati yake kwa Allah, naye ni mwema, na anafuata mila ya Ibrahimu aliyehalisika? Na Allah Amemfanya Ibrahimu kuwa rafiki.

وَمَنْ اَحْسَنُ دِيْنًا مِّمَّنْ اَسْلَمَ وَجْهَهٗ لِلّٰهِ وَهُوَ مُحْسِنٌ وَّاتَّبَعَ مِلَّةَ اِبْرٰهِيْمَ حَنِيْفًا ۭ وَاتَّخَذَ اللّٰهُ اِبْرٰهِيْمَ خَلِيْلًا ﴿١٢٥﴾

127. Na ni vya Allah vilivyomo mbinguni na vilivyomo ardhini; na Allah ndiye Avizungukaye vitu vyote.

وَلِلّٰهِ مَا فِي السَّمٰوٰتِ وَمَا فِي الْاَرْضِ ۭ وَكَانَ اللّٰهُ بِكُلِّ شَيْءٍ مُّحِيْطًا ﴿١٢٦﴾ ع ١٥

FUNGU 19

128. Na wanakuuliza kuhusiana na wanawake. Sema: Allah

وَيَسْتَفْتُوْنَكَ فِي النِّسَاۗءِ ۭ قُلِ اللّٰهُ

Aya 125. *Naqiira* limetafsiriwa "hata kidogo" kwa kufuata mradi wake, lakini maana yake hasa ni kibonde cha kokwa ya tende." Aya hii inawaweka wanawake na wanaume katika usawa kwa mujibu wa matendo yao na malipo.

يُفْتِيكُمْ فِيهِنَّ ۙ وَمَا يُتْلٰى عَلَيْكُمْ فِي
الْكِتٰبِ فِيْ يَتٰمَى النِّسَآءِ الّٰتِيْ لَا تُؤْتُوْنَهُنَّ
مَا كُتِبَ لَهُنَّ وَ تَرْغَبُوْنَ اَنْ تَنْكِحُوْهُنَّ
وَالْمُسْتَضْعَفِيْنَ مِنَ الْوِلْدَانِ ۙ وَاَنْ
تَقُوْمُوْا لِلْيَتٰمٰى بِالْقِسْطِ ؕ وَمَا تَفْعَلُوْا
مِنْ خَيْرٍ فَاِنَّ اللّٰهَ كَانَ بِهٖ عَلِيْمًا ﴿١٢٧﴾

Anawaambieni habari zao, na pia msomewavyo katika Kitabu juu ya wanawake yatima ambao hamwapi (mahari zao) walizoandikiwa, nanyi mnapenda kuwaoa; na juu ya walio dhaifu katika watoto, na (Anawaambieni) ya kwamba jitahidini kuwatendea yatima kwa uadilifu; na wema wo wote mnaofanya, basi Allah Anaujua.

وَاِنِ امْرَاَةٌ خَافَتْ مِنْۢ بَعْلِهَا نُشُوْزًا
اَوْ اِعْرَاضًا فَلَا جُنَاحَ عَلَيْهِمَآ اَنْ
يُّصْلِحَا بَيْنَهُمَا صُلْحًا ؕ وَالصُّلْحُ خَيْرٌ ؕ
وَاُحْضِرَتِ الْاَنْفُسُ الشُّحَّ ؕ وَاِنْ تُحْسِنُوْا
وَتَتَّقُوْا فَاِنَّ اللّٰهَ كَانَ بِمَا تَعْمَلُوْنَ خَبِيْرًا ﴿١٢٨﴾

129. Na kama mke akiogopa kwa mume wake kugombanagombana na kutenganatengana, basi si vibaya kujirekebisha kwa kufanya suluhu; maana suluhu ni bora. Na ubakhili umewekwa ndani ya nafsi; lakini kama mkifanya hisani na kushika ucha Mungu, basi bila shaka Allah Anazo habari za mnayoyatenda.

وَلَنْ تَسْتَطِيْعُوْٓا اَنْ تَعْدِلُوْا بَيْنَ النِّسَآءِ
وَلَوْ حَرَصْتُمْ فَلَا تَمِيْلُوْا كُلَّ الْمَيْلِ
فَتَذَرُوْهَا كَالْمُعَلَّقَةِ ؕ وَاِنْ تُصْلِحُوْا
وَتَتَّقُوْا فَاِنَّ اللّٰهَ كَانَ غَفُوْرًا رَّحِيْمًا ﴿١٢٩﴾

130. Nanyi hamwezi kufanya uadilifu uliokamilika baina ya wake, hata kama mngependa namna gani. Kwa hiyo msiegemee moja kwa moja kwa mke mmoja isije mkamuacha mwingine kama aliyeangikwa, (asiyehudumiwa na asiyeangaliwa). Lakini kama ninyi mkijirekebisha na kujilinda na uovu, basi hakika Allah ni Msamehevu, Mrehemevu.

Aya 129. *Nafsi zimewekewa tamaa mbele yao*. Maneno hayo yanaonyesha sababu hasa za ugomvi unaotokea kati ya mume na mke. Zinaweza kusemwa ni choyo au ubahili wa mume na tamaa ya mke. Mume anapokuwa hampendi mke wake huona anelemewa kumpa matumizi. Upande mwingine mke huenda akaombaomba mno kwa mume wake. Aya inawapa mauidha wote watendeane kwa uadilifu na kwa haki.

Aya 130. *Kal-mu'allaqah* "Kama aliyeangikwa." *Mu'allaqah* ni mke ambaye mumewe hamweki vyema na wala hampi talaka apate kuolewa na mwanamume mwingine (Lane na Akarb).

Nanyi hamwezi kufanya adili baina ya wake. Bi Aisha mama wa waaminio, mkewe Mtume *s.a.w.* anasimulia ya kwamba Mtume *s.a.w.* alikuwa akiwatendea wakeze sawasawa katika mambo yote yaliyo katika uwezo wake na baada ya kufanya hivi alikuwa akiomba kwa Allah

وَاِنْ يَّتَفَرَّقَا يُغْنِ اللّٰهُ كُلًّا مِّنْ سَعَتِهٖ ؕ
وَكَانَ اللّٰهُ وَاسِعًا حَكِيْمًا ﴿١٣٠﴾

131. Na kama wakitengana, Allah Atamstawisha kila mmoja wao kwa wasaa Wake, na Allah ni Mwenye wasaa, Mwenye hekima.

وَلِلّٰهِ مَا فِي السَّمٰوٰتِ وَمَا فِي الْاَرْضِ ؕ
وَلَقَدْ وَصَّيْنَا الَّذِيْنَ اُوْتُوا الْكِتٰبَ مِنْ
قَبْلِكُمْ وَاِيَّاكُمْ اَنِ اتَّقُوا اللّٰهَ ؕ وَاِنْ
تَكْفُرُوْا فَاِنَّ لِلّٰهِ مَا فِي السَّمٰوٰتِ وَمَا فِي
الْاَرْضِ ؕ وَكَانَ اللّٰهُ غَنِيًّا حَمِيْدًا ﴿١٣١﴾

132. Na ni vya Allah vilivyomo mbinguni na vilivyomo ardhini. Na kwa yakini Tuliwaagiza waliopewa Kitabu kabla yenu, na ninyi pia, ya kwamba mumche Allah. Na kama mkikataa, basi ni vya Allah vilivyomo mbinguni na vilivyomo ardhini, na Allah ni Mkwasi, Asifiwaye.

وَلِلّٰهِ مَا فِي السَّمٰوٰتِ وَمَا فِي الْاَرْضِ ؕ
وَكَفٰى بِاللّٰهِ وَكِيْلًا ﴿١٣٢﴾

133. Na vyote vilivyomo mbinguni na vilivyomo ardhini ni vya Allah; na Allah Anatosha kuwa Mlinzi.

اِنْ يَّشَاْ يُذْهِبْكُمْ اَيُّهَا النَّاسُ وَيَاْتِ
بِاٰخَرِيْنَ ؕ وَكَانَ اللّٰهُ عَلٰى ذٰلِكَ قَدِيْرًا ﴿١٣٣﴾

134. Kama akipenda Atawaondoeni enyi watu, na Atawaleta wengine; na Allah ni Mweza wa hayo.

مَنْ كَانَ يُرِيْدُ ثَوَابَ الدُّنْيَا فَعِنْدَ اللّٰهِ
ثَوَابُ الدُّنْيَا وَالْاٰخِرَةِ ؕ وَكَانَ اللّٰهُ
سَمِيْعًا بَصِيْرًا ﴿١٣٤﴾ ع ١٦

135. Anayetaka malipo ya dunia, basi yako kwa Allah malipo ya dunia na pia ya Akhera. Na Allah ni Mwenye kusikia, Mwenye kuona.

akisema, "Mola wangu, hivi ndivyo nitendavyo katika mambo ninayoweza; basi usinilaumu kwa yale yaliyo katika uwezo Wako ambayo mimi siyawezi," yaani maoni ya moyo (Dawud, sura *Nikaah*). Tena Mtume *s.a.w.* akasema, "Kama mtu anao wake wawili na anaelekea kwa mmoja (na kutomjali mwingine) atafufuliwa siku ya Kufufuka na ubavu wake mmoja umechanwa" (Dawua sura *Nikaah)*. Hivyo hadithi hizi mbili za Mtume *s.a.w*. zinaonyesha ya kwamba ingawa mume hawezi kuwapenda wakeze sawasawa lakini lazima katika matendo ya nje, kama kuwapa matumizi na wakati, awatendee wote sawasawa.

Aya 131. Inapokuwa mke na mume wameshindwa kabisa kuendelea maisha yao pamoja, basi jambo lililo zuri kwao ni kwamba watengane; na Allah Ameahidi kumnufaisha kila mmoja kwa kumpatia mwenzi wa kumfaa. Jinsi Islam inavyoona jambo la mke na mume kuachana ni kama inavyoonekana katika Hadithi ya Mtume *s.a.w*. isemayo, "Hakika jambo la halali linalochukiza sana mbele ya Allah ni talaka" (Dawud sura *Talaak*).

FUNGU 20

يٰٓاَيُّهَا الَّذِيْنَ اٰمَنُوْا كُوْنُوْا قَوّٰمِيْنَ بِالْقِسْطِ
شُهَدَآءَ لِلّٰهِ وَلَوْ عَلٰٓى اَنْفُسِكُمْ اَوِ
الْوَالِدَيْنِ وَالْاَقْرَبِيْنَ ۚ اِنْ يَّكُنْ غَنِيًّا اَوْ
فَقِيْرًا فَاللّٰهُ اَوْلٰى بِهِمَا ۣ فَلَا تَتَّبِعُوا
الْهَوٰٓى اَنْ تَعْدِلُوْا ۚ وَاِنْ تَلْوٗٓا اَوْ تُعْرِضُوْا
فَاِنَّ اللّٰهَ كَانَ بِمَا تَعْمَلُوْنَ خَبِيْرًا ﴿١٣٥﴾

136. Enyi mlioamini! Kuweni wenye kusimamia uadilifu, mkiwa mashahidi kwa ajili ya Allah, hata kama jambo husika liwe dhidi ya nafsi zenu, au (juu ya) wazazi (wenu) na jamaa wa karibu. Kama akiwa tajiri au maskini Allah Yu karibu nao zaidi wote wawili. Basi msifuate matamanio ili kutofanya uadilifu. Na kama mkipotosha (ukweli) au mkijitenga, basi hakika Allah Anazo habari za mnayoyatenda.

يٰٓاَيُّهَا الَّذِيْنَ اٰمَنُوْٓا اٰمِنُوْا بِاللّٰهِ وَرَسُوْلِهٖ
وَالْكِتٰبِ الَّذِيْ نَزَّلَ عَلٰى رَسُوْلِهٖ
وَالْكِتٰبِ الَّذِيْٓ اَنْزَلَ مِنْ قَبْلُ ۭ وَمَنْ
يَّكْفُرْ بِاللّٰهِ وَمَلٰۗىِٕكَتِهٖ وَكُتُبِهٖ وَرُسُلِهٖ
وَالْيَوْمِ الْاٰخِرِ فَقَدْ ضَلَّ ضَلٰلًۢا بَعِيْدًا ﴿١٣٦﴾

137. Enyi mlioamini! mwaminini Allah na Mtume Wake, na Kitabu Alichokiteremsha juu ya Mtume Wake, na Kitabu Alichokiteremsha zamani; na mwenye kumkataa Allah na Malaika Wake na Vitabu Vyake na Mitume Wake na Siku ya Mwisho, basi bila shaka amepotea upotevu wa mbali.

اِنَّ الَّذِيْنَ اٰمَنُوْا ثُمَّ كَفَرُوْا ثُمَّ اٰمَنُوْا ثُمَّ
كَفَرُوْا ثُمَّ ازْدَادُوْا كُفْرًا لَّمْ يَكُنِ اللّٰهُ
لِيَغْفِرَ لَهُمْ وَلَا لِيَهْدِيَهُمْ سَبِيْلًا ﴿١٣٧﴾

138. Hakika wale walioamini kisha wakakufuru, kisha wakaamini, kisha wakakufuru, tena wakazidi katika kufuru, Allah Hatawasamehe wala Hatakuwa Mwenye kuwaongoza njia.

بَشِّرِ الْمُنٰفِقِيْنَ بِاَنَّ لَهُمْ عَذَابًا اَلِيْمَۨا ﴿١٣٨﴾

139. Wabashirie wanafiki ya kwamba watapata adhabu iumizayo,

Aya 136. *Ijapokuwa ni juu ya nafsi zenu.* Maneno haya pia yanaweza kufasiriwa, *Ijapokuwa ni juu ya watu wenu au juu ya ndugu zenu.* Maneno, *wazazi (wenu) na jamaa wa karibu* yameongezwa kutia mkazo ya kuwa ushahidi wa kweli ni jambo la lazima kabisa hata kama ushahidi huo uwe unaomdhuru baba wa mtu na nduguze au jamaa zake.

Aya 138. *Walioamini, kisha wakakufuru.* Wako watu wanaosema ya kuwa, kama mtu anaacha dini baada ya kuamini, basi kufuru yake hii inamstahilisha kupata adhabu ya kuuawa. Lakini Aya hii inavunja kabisa wazo la namna hii, maana sheria hiyo ingekuwa katika dini ya Kiislamu kuwa anayeacha dini auawe, watu wasingeweza kupata nafasi ya kuamini kisha kukufuru na kuamini tena na kisha kukufuru na kisha kuzidi katika kufuru.

الَّذِيْنَ يَتَّخِذُوْنَ الْكٰفِرِيْنَ اَوْلِيَآءَ مِنْ
دُوْنِ الْمُؤْمِنِيْنَ ؕ اَيَبْتَغُوْنَ عِنْدَهُمُ
الْعِزَّةَ فَاِنَّ الْعِزَّةَ لِلّٰهِ جَمِيْعًا ﴿١٣٩﴾

140. Ambao huwafanya makafiri kuwa marafiki badala ya waaminio, Je, wanataka wapate heshima kwao? Basi hakika heshima yote ni ya Allah.

وَقَدْ نَزَّلَ عَلَيْكُمْ فِي الْكِتٰبِ اَنْ اِذَا
سَمِعْتُمْ اٰيٰتِ اللّٰهِ يُكْفَرُ بِهَا وَيُسْتَهْزَاُ بِهَا
فَلَا تَقْعُدُوْا مَعَهُمْ حَتّٰى يَخُوْضُوْا فِيْ
حَدِيْثٍ غَيْرِهٖۤ ۚ اِنَّكُمْ اِذًا مِّثْلُهُمْ ؕ اِنَّ
اللّٰهَ جَامِعُ الْمُنٰفِقِيْنَ وَالْكٰفِرِيْنَ
فِيْ جَهَنَّمَ جَمِيْعًا ۙ﴿١٤٠﴾

141. Naye Amekwisha wateremshieni katika Kitabu ya kwamba mnaposikia Aya za Allah zinakataliwa na kufanyiwa mzaha, basi msikae pamoja nao, mpaka waingie katika mazungumzo ghairi ya hayo; (maana mkiendelea kukaa) hakika ndipo mtakuwa kama wao. Hakika Allah Atawakusanya wanafiki na makafiri wote katika Jahanamu;

الَّذِيْنَ يَتَرَبَّصُوْنَ بِكُمْ ۚ فَاِنْ كَانَ لَكُمْ
فَتْحٌ مِّنَ اللّٰهِ قَالُوْۤا اَلَمْ نَكُنْ مَّعَكُمْ ۖۗ
وَاِنْ كَانَ لِلْكٰفِرِيْنَ نَصِيْبٌ ۙ قَالُوْۤا اَلَمْ
نَسْتَحْوِذْ عَلَيْكُمْ وَنَمْنَعْكُمْ مِّنَ
الْمُؤْمِنِيْنَ ؕ فَاللّٰهُ يَحْكُمُ بَيْنَكُمْ يَوْمَ
الْقِيٰمَةِ ؕ وَلَنْ يَّجْعَلَ اللّٰهُ لِلْكٰفِرِيْنَ عَلَى
الْمُؤْمِنِيْنَ سَبِيْلًا ﴿١٤١﴾ ع ١٧

142. Ambao wanawangojeeni (mpate msiba); basi kama mkipata ushindi kutoka kwa Allah, husema: Je! hatukuwa pamoja nanyi? Na kama makafiri wakipata sehemu, husema: Je, hatukuwashindeni na kuwalindeni na waaminio? Basi Allah Atahukumu baina yenu Siku ya Kiyama; na Allah hatawajaalia makafiri njia ya kuwashinda waaminio.

FUNGU 21

اِنَّ الْمُنٰفِقِيْنَ يُخٰدِعُوْنَ اللّٰهَ وَهُوَ
خَادِعُهُمْ ۚ وَاِذَا قَامُوْۤا اِلَى الصَّلٰوةِ
قَامُوْا كُسَالٰى ۙ يُرَآءُوْنَ النَّاسَ وَلَا
يَذْكُرُوْنَ اللّٰهَ اِلَّا قَلِيْلًا ﴿١٤٢﴾

143. Hakika wanafiki wanataka kumdanganya Allah, lakini Yeye Atawasababisha wajidanganye wenyewe; nao wanaposimama kusali, husimama kwa uvivu, hujionyesha kwa watu wala hawamkumbuki Allah ila kidogo tu;

Aya 143 na **144** Zinaeleza waziwazi alama za wanafiki. Mtume *s.a.w.* amesema. "Sala iliyo nzito mno kwa wanafiki ni Sala ya Alasiri, Ishaa na ya Alfajiri," "Mnafiki hungoja mpaka

مُّذَبْذَبِيْنَ بَيْنَ ذٰلِكَ ۖ لَآ اِلٰى هٰٓؤُلَآءِ وَلَآ اِلٰى هٰٓؤُلَآءِ ۭ وَمَنْ يُّضْلِلِ اللّٰهُ فَلَنْ تَجِدَ لَهٗ سَبِيْلًا ﴿١٤٣﴾

144. Wakisitasita baina ya hayo. huku hawako wala huku hawako. Na ambaye Allah amemhukumu kupotea, basi huwezi kumpatia njia.

يٰٓاَيُّهَا الَّذِيْنَ اٰمَنُوْا لَا تَتَّخِذُوا الْكٰفِرِيْنَ اَوْلِيَاۗءَ مِنْ دُوْنِ الْمُؤْمِنِيْنَ ۭ اَتُرِيْدُوْنَ اَنْ تَجْعَلُوْا لِلّٰهِ عَلَيْكُمْ سُلْطٰنًا مُّبِيْنًا ﴿١٤٤﴾

145. Enyi mlioamini, msiwafanye makafiri kuwa marafiki badala ya waaminio; je, mnataka kumpa Allah dalili dhahiri juu yenu?

اِنَّ الْمُنٰفِقِيْنَ فِي الدَّرْكِ الْاَسْفَلِ مِنَ النَّارِ ۚ وَلَنْ تَجِدَ لَهُمْ نَصِيْرًا ﴿١٤٥﴾ۙ

146. Bila shaka wanafiki wako katika daraja la chini la Moto, wala hutakuta kwa ajili yao msaidizi ye yote.

اِلَّا الَّذِيْنَ تَابُوْا وَاَصْلَحُوْا وَاعْتَصَمُوْا بِاللّٰهِ وَاَخْلَصُوْا دِيْنَهُمْ لِلّٰهِ فَاُولٰۗىِٕكَ مَعَ الْمُؤْمِنِيْنَ ۭ وَسَوْفَ يُؤْتِ اللّٰهُ الْمُؤْمِنِيْنَ اَجْرًا عَظِيْمًا ﴿١٤٦﴾

147. Isipokuwa wale wanaotubu na kujisahihisha na kumshika Allah, na kuuhalisisha utii wao kwa Allah, basi hao wako pamoja na waaminio. Na Allah karibuni Atawapa waaminio ujira mkuu.

مَا يَفْعَلُ اللّٰهُ بِعَذَابِكُمْ اِنْ شَكَرْتُمْ وَاٰمَنْتُمْ ۭ وَكَانَ اللّٰهُ شَاكِرًا عَلِيْمًا ﴿١٤٧﴾

148. Allah ana haja gani kuwaadhibuni kama mkishukuru na kuamini? Na Allah ndiye Mwenye kupokea shukurani Mwenye kujua.

jua linakaribia kutua ndipo husimama na akasali haraka-haraka rakaa nne za Sala ya Alasiri na kumkumbuka Mwenyezi Mungu kidogo" (Muslim); na katika Bukhari, imesemwa ni Sala za Alfajiri na Ishaa.

Aya 145. Mtu anayefanya urafiki na makafiri wakati makafiri wako katika vita na Waislamu yeye anasaidia kufuru, na ni lazima atajiteremshia ghadhabu ya Allah.

Aya 146. *Wako katika daraja ya chini ya Moto.* Maana wamechanganya dhambi ya kufuru na ya unafiki. Katika Islam wanafiki wamelaumiwa sana hata kuliko makafiri, maana wao ndio sababu ya kukuza fitina za namna mbalimbali katika umati wa watu.

Aya 147. *Wako pamoja na waaminio.* Sio mradi wake kuwa wao hawatakuwa waaminio, bali wao pia watakuwa waaminio. *Ma'a* hii ndio kama ile iliyotumika katika sura 4:70.

Aya 148. *Kama mtashukuru.* Neno la *shukr* linapotumiwa kwa ajili ya mtu ni kujali neema za Allah, na kutoa shukurani kwa matamko na kwa matendo; na kwa upande wa Allah lina maana ya kutoa malipo yanayostahili kupewa watu kwa ajili ya utii wao na wema wao.

JUZU 6

لَا يُحِبُّ اللّٰهُ الْجَهْرَ بِالسُّوْٓءِ مِنَ الْقَوْلِ اِلَّا مَنْ ظُلِمَ ؕ وَكَانَ اللّٰهُ سَمِيْعًا عَلِيْمًا ﴿۱۴۸﴾

149. Allah hapendi jambo baya lisemwe hadharani ila kwa yule aliyedhulumiwa; na Allah ndiye Asikiaye, Ajuaye.

اِنْ تُبْدُوْا خَيْرًا اَوْ تُخْفُوْهُ اَوْ تَعْفُوْا عَنْ سُوْٓءٍ فَاِنَّ اللّٰهَ كَانَ عَفُوًّا قَدِيْرًا ﴿۱۴۹﴾

150. Mkidhihirisha wema au mkiuficha, au mkiyasamehe maovu, basi hakika Allah ni Msamehevu, Mwenye kuweza.

اِنَّ الَّذِيْنَ يَكْفُرُوْنَ بِاللّٰهِ وَرُسُلِهٖ وَيُرِيْدُوْنَ اَنْ يُّفَرِّقُوْا بَيْنَ اللّٰهِ وَرُسُلِهٖ وَيَقُوْلُوْنَ نُؤْمِنُ بِبَعْضٍ وَّنَكْفُرُ بِبَعْضٍ ۙ وَّيُرِيْدُوْنَ اَنْ يَّتَّخِذُوْا بَيْنَ ذٰلِكَ سَبِيْلًا ۙ ﴿۱۵۰﴾

151. Hakika wale wanaomkataa Allah na Mitume Wake, na wanataka kutofautisha baina ya Allah na Mitume Wake, na husema: Wengine tunawaamini na wengine tunawakataa, na wanataka kushika njia iliyo kati ya haya,

اُولٰٓئِكَ هُمُ الْكٰفِرُوْنَ حَقًّا ۚ وَاَعْتَدْنَا لِلْكٰفِرِيْنَ عَذَابًا مُّهِيْنًا ﴿۱۵۱﴾

152. Hao ndio makafiri kweli, na Tumewaandalia makafiri adhabu ifedheheshayo.

وَالَّذِيْنَ اٰمَنُوْا بِاللّٰهِ وَرُسُلِهٖ وَلَمْ يُفَرِّقُوْا بَيْنَ اَحَدٍ مِّنْهُمْ اُولٰٓئِكَ سَوْفَ يُؤْتِيْهِمْ اُجُوْرَهُمْ ؕ وَكَانَ اللّٰهُ غَفُوْرًا رَّحِيْمًا ﴿۱۵۲﴾ ع ۲۱

153. Na waliomwamini Allah na Mitume Wake, wala hawakumfarikisha mmojawapo kati yao, hao ndio karibuni Atawapa ujira wao. Na Allah ni Msamehevu, Mrehemevu.

Aya 149. Dini ya Kiislamu haimruhusu kumsema mtu vibaya mbele za watu, lakini mtu anayedhulumiwa anaweza kupiga kelele wakati anapokuwa anadhulumiwa ili watu wengine wafike kumsaidia. Kadhalika anaweza kushtaki mahakamani. Lakini asipitepite akinung'unika kwa kila mtu, maana jambo hili linaweza kuleta ghasia na kuharibu amani, na Qur'an haitaki jambo la namna hii.

Aya 151. Ibni Kathir, mfasiri anayesifikana wa Qur'an anaieleza Aya hii hivi: "Mradi hapa ni kwamba mtu anayemkataa Mtume ye yote wa Allah, kwa hakika anawakataa wote; maana Allah Amemlazimisha mwanadamu kumkubali kila Mtume aliyepelekwa kwa taifa lo lote wakati wo wote" (jalada iii, 224). Kwa hakika kama watu wanamkataa Nabii wa Allah kwa sababu ya kijicho au ushupavu na ukaidi, inakuwa ni wazi ya kuwa imani yao juu ya Mtume wanayesema wanamwamini si ya dhati, bali ni ya kujisingizia tu. Maana kama wangemwamini kuwa yu Mtume wa Mungu kweli, bila shaka wangemwamini yule mwingine ambaye pia amefanana naye na ambaye amehakikishwa kwa hoja zile zile.

FUNGU 22

يَسْـَٔلُكَ اَهْلُ الْكِتٰبِ اَنْ تُنَزِّلَ عَلَيْهِمْ
كِتٰبًا مِّنَ السَّمَآءِ فَقَدْ سَاَلُوْا مُوْسٰٓى اَكْبَرَ
مِنْ ذٰلِكَ فَقَالُوْٓا اَرِنَا اللّٰهَ جَهْرَةً فَاَخَذَتْهُمُ
الصّٰعِقَةُ بِظُلْمِهِمْ ۚ ثُمَّ اتَّخَذُوا الْعِجْلَ
مِنْۢ بَعْدِ مَا جَآءَتْهُمُ الْبَيِّنٰتُ فَعَفَوْنَا عَنْ
ذٰلِكَ ۚ وَاٰتَيْنَا مُوْسٰى سُلْطٰنًا مُّبِيْنًا ﴿١٥٣﴾

154. Watu wa Kitabu wanakuomba ya kwamba uwateremshie Kitabu kutoka mbinguni. Na kwa hakika walimwomba Musa makubwa kuliko hayo, na wakasema: Utuonyeshe Mungu waziwazi. Ndipo ikawashika ngurumo ya radi kwa sababu ya dhuluma yao. Kisha wakamshika ndama (kuwa mungu) baada ya kuwafikia ishara zilizo wazi; lakini Tukasamehe hayo na Tukampa Musa dalili iliyo dhahiri.

وَرَفَعْنَا فَوْقَهُمُ الطُّوْرَ بِمِيْثَاقِهِمْ وَقُلْنَا
لَهُمُ ادْخُلُوا الْبَابَ سُجَّدًا وَّ قُلْنَا لَهُمْ
لَا تَعْدُوْا فِى السَّبْتِ وَاَخَذْنَا مِنْهُمْ
مِّيْثَاقًا غَلِيْظًا ﴿١٥٤﴾

155. Na Tukaunyanyua mlima juu yao kwa kufanya agano nao, Tukawaambia, ingieni mlangoni hali ya kutii, na pia Tukawaambia: Msiruke mipaka ya Sabato, na Tukashika kwao ahadi iliyo madhubuti.

فَبِمَا نَقْضِهِمْ مِّيْثَاقَهُمْ وَكُفْرِهِمْ بِاٰيٰتِ
اللّٰهِ وَقَتْلِهِمُ الْاَنْۢبِيَآءَ بِغَيْرِ حَقٍّ وَّقَوْلِهِمْ
قُلُوْبُنَا غُلْفٌ ؕ بَلْ طَبَعَ اللّٰهُ عَلَيْهَا
بِكُفْرِهِمْ فَلَا يُؤْمِنُوْنَ اِلَّا قَلِيْلًا ﴿١٥٥﴾

156. Basi kwa sababu ya kuvunja kwao ahadi yao, na kuzikataa kwao Ishara za Allah, na kuua kwao Manabii bila ya haki, na kwa kusema kwao, mioyo yetu imefunikwa; bali Allah Aliipiga muhuri kwa kufuru zao, kwa hiyo hawaamini ila kidogo tu.

وَّبِكُفْرِهِمْ وَقَوْلِهِمْ عَلٰى مَرْيَمَ
بُهْتَانًا عَظِيْمًا ﴿١٥٦﴾

157. Na kwa sababu ya kufuru zao na kusema kwao juu ya Mariamu masingizio makubwa.

Aya 157. *Masingizio makubwa.* Mayahudi kumsingizia sana Mariamu ni ushahidi ulio wazi ya kuwa Nabii Isa alikuwa hana baba, basi ni masingizio gani Mayahudi waliyomsingizia Mariamu? Mahali pengine Qur'an inasema kuwa mama wa Nabii Isa alikuwa mwanamke mcha Mungu na ya kuwa kuzaliwa kwa Nabii Isa hakukuwa kwa kishetani (sura 3:37; na 5:76).

158. Na kusema kwao: Hakika tumemwua Masihi Isa mwana wa Mariamu, Mtume wa Mungu; hali hawakumwua wala hawakumfisha msalabani, bali alifananishwa kwao (kama maiti). Na kwa hakika wale waliohitilafiana kwalo, yakini wana shaka nalo, wao hawalijui hakika yake isipokuwa wanafuata dhana. Na kwa yakini wao hawakumwua–

وَّقَوْلِهِمْ اِنَّا قَتَلْنَا الْمَسِيْحَ عِيْسَى ابْنَ
مَرْيَمَ رَسُوْلَ اللّٰهِ ۚ وَمَا قَتَلُوْهُ وَمَا
صَلَبُوْهُ وَلٰكِنْ شُبِّهَ لَهُمْ ؕ وَاِنَّ الَّذِيْنَ
اخْتَلَفُوْا فِيْهِ لَفِيْ شَكٍّ مِّنْهُ ؕ مَا لَهُمْ بِهٖ مِنْ
عِلْمٍ اِلَّا اتِّبَاعَ الظَّنِّ ۚ وَمَا قَتَلُوْهُ يَقِيْنًا ۙ﴿۱۵۷﴾

Aya 158. *Wamaa salabuuhu,* "Wala hawakumfisha msalabani." Baadhi ya watu hufasiri neno hili kuwa "hawakumsulubu," kwa maana ya kuwa Nabii Isa hata hakupigiliwa msalabani. Sivyo. Neno hili maana yake ni "kuua kwa kupigilia na kufunga mtini." (Lane na Akrab). Hivyo tumelifasiri "hawakumfisha msalabani," ingawa alipigiliwa hasa msalabani , ila tu hakufa juu ya msalaba.

Msisitizo umo katika kushindwa kwao kumwua Yesu kwa kila njia. Msomaji anakumbushwa kwamba mwanzo kabisa wa aya hii unarejea kujigamba kwa Mayahudi kwamba walikuwa wamefanikiwa katika kumwua Yesu.

Dai hili la Mayahudi linakataliwa kwa nguvu zote na Qur'an Tukufu. Hii ndiyo sababu mwishoni mwa aya hii, tangazo la kukata hukumu ni hili ya kwamba cho chote kile ambacho chaweza kuwa kimetokea kwa hakika wao walishindwa kumwua. Hii inaashiria kwamba kinachokanushwa hapa siyo kitendo cha kumsulubu. Kinachokanushwa ni kifo kwa njia ya kusulubishwa.

Walaakin shubbiha lahum. Neno *shubbiha* katika maandiko haya ni lazima lichunguzwe kwa uangalifu. Maudhui ya maandiko yaliyotangulia yasingeruhusu marejeo yanayoashiriwa kwa mtu mwingine ye yote asiyekuwa Yesu au vinginevo yangelirejea tukio lenyewe kwa ujumla. Kwa kuzingatia kanuni za sarufi, kijina kinachoashiriwa katika neno *shubbiha* chaweza kurejea si kwa mwingine isipokuwa Yesu Kristo mwenyewe. Hii ina maana kwamba ni yeye aliyekuwa amefichika na kufanywa aonekane kwao katika hali nyingine. Hivyo basi Yesu alipotundikwa msalabani alining'inia akifanana na mtu aliyekufa. Ni dhahiri kwamba kanusho siyo lile la kupachikwa msalabani au kilichoonekana kama kifo pale juu bali kanusho lenyewe linahusu kifo kwa njia ya kusulubishwa. Bila shaka kulikuweko na kutofahamu kuhusu nini hasa kilichotokea. Kwa hiyo aya hii inaendelea kujenga mpangilio wa matukio ya hali hiyo ya kutofahamu na shaka. Mengine yote si cho chote ila dhana tu. Huo ndio uamuzi wa mwisho.

Kama neno *shubbiha* linarejea tukio kama lilivyo, hii itaashiria kwenye madai yanayotaofutiana ya pande mbili zinazohitilafiana kuhusu nini kilitokea. Hakuna kundi moja kati ya hayo mawili lililokuwa na uhakika kuhusu madai yake. Kwa mfano imani ya Kikristo kuhusu kifo cha Yesu kwa njia ya kusulubiwa na hatimae kufufuka haikujengwa juu ya misingi yo yote ya maana bali ilikuwa ya kudhania tu. Kadhalika dai la Mayahudi kuhusu kifo cha Yesu juu ya msalaba halikuwa isipokuwa la kudhania tu. Ndiyo sababu walimsihi Pilato awakabidhi mwili wa Yesu. Kwa hakika walionyesha waziwazi shaka yao kuhusu hadithi zote za kilichoitwa kifo chake na wakamwonya Pilato kwamba endapo ataepukana na kifo huenda atajitokeza hadharani akidai kwamba amefufuka kutoka katika wafu (Mathayo 27:63:64).

Hiki ndicho kinachorejewa na sehemu ya mwisho ya aya husika inaposema: *"Wainnaladhiina ....."* kwa hakika wale wanaohitilafiana kuhusu jambo hili (au kumhusu yeye ni nini hasa kilichomsibu) wao wenyewe wamo katika shaka.

Bal Rafa'ahullaahu ilaihi Wengi miongoni mwa Waislamu muhaafidhiina huonelea kutokana na sehemu hii ya aya kwamba hiki kiambishi *bal* kinarejea kitendo cha usulubishaji, yaani, badala ya kumwacha afe juu ya msalaba Allah alimwokoa kwa kumnyanyua kimwili hadi mahali fulani huko mbinguni. Hivyo basi ni lazima awe anaishi mahali fulani angani katika hali ile ile ya kimwili aliyokuwa nayo kabla ya jaribio la kusulubiwa kwake. Tafsiri hii inaleta maswali mengi magumu, hususan:

(a) Kama Yesu hakusulubiwa kabisa, jee hii historia nzima ya kusulubisha inakanushwa vikali na kwamba mlolongo wote wa hadithi hizi ni kisa tu kilichotungwa au kupangwa kulikowakumba Wayahudi, Wakristo na Warumi kwa mpigo?

(b) Ni wapi katika aya hii penye dai kwamba Yesu alinyanyuliwa kimwili kwenda mbinguni? Kinachotajwa ni hiki tu ya kwamba Allah Alimnyanyua Kwake.

Kuhusu swali la kwanza walio muhafidhiina wanajenga mpangilio wa matukio wa kuchekesha ambao kulingana na huo, ukweli wenyewe kuhusu kusulubishwa haukanushwi bali inadaiwa kwamba yule mtu aliyesulubishwa hakuwa Yesu bali mtu mwingine ambaye baadhi ya malaika walimpa umbile la Yesu kwa amri ya Allah. Kwa hiyo zile shaka na dhana zilihusiana na utambulisho wa yule mtu aliyesulubiwa. Ni dhahiri kwamba maelezo haya yanaleta utatanishi mwingi tu kuliko utatuzi. Isitoshe kisa chote hakina msingi kabisa. Hakuna ushahidi wa maandiko matakatifu au ushahidi ambao msingi wake ni Hadithi za Mtukufu Mtume s.a.w. uliopata kutolewa ili kuunga mkono dai hili la kichekesho ambalo linazidisha tu dukuduku la dhana.

Ni kana kwamba maelezo haya ya aya hii yaliwapambazukia wanazuoni wa kale tu, wakati Mtume wa Allah mwenyewe amani juu yake alibakia asiyejua lo lote juu ya jambo hili.

Kuhusu swali la pili udhaifu wa dai hilo unaonekana kutokana na muundo wa maneno ya Qur'an Tukufu. Neno *rafa'a* lina maana ya kunyanyua. Kila Allah anapomnyanyua mtu kunyanyua huko kila mara kunamaanisha hadhi ya mtu yule na kamwe hakumaanishi mwili wake. Kwa hakika haiwezekani kuitafsiri aya hii kwa njia nyingine yo yote kinyume cha maana hiyo iliyosemwa, yaani kunyanyuliwa kwa cheo cha kiroho.

Aya hii inatangaza kwamba Allah Alimnyanyua Yesu Kwake. Kidhahiri hakuna nukta katika anga la mbinguni panapotajwa kuwa ndipo alipowekwa wakati Allah Alipomnyanyua. Alimnyanyua Kwake kwa hali ya kwamba Alikuwapo pale pale alipokuwa Yesu. Hakuna mahali mbinguni au ardhini ambapo pako tupu kwa maana ya kwamba Allah hayupo hapo. Kwa hiyo mtu anaposemekana kuwa amenyanyuliwa Kwake, mwenendo wa kimwili ni jambo lisilowezekana na lisiloingia akilini. Kulingana na uelewa wa Kiahmadiyya wa aya hii, hiki kiambishi cha *kinyume* kinalirejea dai la Mayahudi la kifo cha laana cha Yesu. Ni wazi kwamba kinyume cha laana ni ukaribu kwa Allah.

Kwa neno zima, Aya hii inaeleza habari moja iliyotokea katika maisha ya Nabii Isa. Mayahudi walikusudia kumwua juu ya msalaba ili waseme, kwa mujibu wa Taurati (Kumbukumbu 21:23) kuwa amelaaniwa. Allah anaeleza ya kuwa hila hii ya Mayahudi haikufanikiwa, na hawakuweza kumwua Nabii Isa kama walivyokusudia.

Kulielewa jambo hili vizuri tuchungue habari za kupigiliwa Yesu msalabani zilizoelezwa katika Agano Jipya.

Ingawa Yesu alitumwa na Mungu, Mayahudi hawakutaka kumsadiki, na walimwona kama ni mwongo tu, na wakajaribu kumwua msalabani ili kuhakikisha kuwa ni mtu aliyelaaniwa.

1. YESU ALIOMBA AEPUSHWE NA KIFO KIBAYA

Yesu, zisemavyo Injili, aliomba sana kwa Allah aepushwe na kifo cha laana. Alikesha usiku akiomba na akiwaambia wanafunzi wake pia waombe kwa Allah.

Yesu alianguka kifudifudi akaomba, "Abba, Baba, yote yanawezekana kwako; uniondolee kikombe hiki; walakini, si nitakavyo mimi, bali utakavyo wewe" (Marko 14:36). "Si nitakavyo mimi." Yesu angejua kuwa kufa kwake msalabani ndiyo mapendeleo ya Allah, asingeomba, "Yote yanawezekana kwako; uniondolee kikombe hiki," yaani kikombe cha mauti, maadui zake walichokusudia kumnywesha.

Juu ya kupokelewa maombi ya Yesu, tunasoma, "Ni mengi maovu yampatayo mwenye haki lakini Mungu humponya nayo yote. Yeye hulinda mifupa yake yote: usivunjike hata mmoja" (Zaburi 34:19, 20). Na Yesu mwenyewe anakiri ya kuwa Mungu daima huzisikia dua zake. Anasema, "Baba, nakushukuru kwa kuwa umenisikia. Nami nilijua ya kuwa wewe wanisikia siku zote" (Yohana 11:42).

Hivyo, ni salama kusema ya kuwa maombi ya Yesu, aliyoomba kuepushwa na kifo cha msalaba, yalipokelewa na Allah. Nasi, tunapochungua habari hii nzima katika Agano Jipya, tunaona wazi kudura ya Allah ikipita kumsalimisha Yesu na mauti yale ya aibu.

2. MKE WA HAKIMU ALIONA NDOTO.

Hakimu Pilato alipokuwa akisikiliza kesi ya Yesu akapata kujua ya kuwa Yesu alikuwa hana kosa, na ya kwamba yule kuhani mkubwa alimshitaki kwa kumuonea husuda tu. Imeandikwa, "Na alipokuwa ameketi juu ya kiti cha hukumu, mkewe alimpelekea mjumbe, kumwambia usiwe na neno na yule mwenye haki; kwa sababu nimeteswa mengi leo katika ndoto kwa ajili yake" (Matt. 27:18-19). Kama Mungu hakukusudia kumponyesha Yesu, palikuwa na haja gani kumwonyesha mke wa hakimu ndoto ya namna hiyo? Jambo hili linafanana na jinsi Allah alivyomfahamisha Yusuf ndotoni, kumwondoa Yesu na mama yake kuwapeleka Misri, wakati Herod alipotaka kumwua bado angali mtoto (Matt. 2:16-19).

3. PILATO ALITAKA KUMWOKOA YESU

Pilato angependa kumwachia Yesu, lakini aliogopa fitina ya Mayahudi. Juu ya hayo alijitahidi kumsaidia kwa njia nyingine za siri ili asife. Alipanga kumtia msalabani siku ya Ijumaa, na akakawiza hukumu mpaka saa sita (Yohana 19:14) ili kuufupisha muda wa kukaa kwake msalabani. Maana alijua ya kuwa ni haramu kwa Mayahudi kuacha miili juu ya msalaba usiku wa kuamkia Jumamosi, iliyo ni siku yao ya ibada ya Sabato. Yesu hajakaa sana msalabani, inasemekana kukawa giza katika nchi (Marko 15:33), ardhi ikatetemeka na pazia la hekalu likapasuka mapande mawili (Matt. 27:51). Matokeo haya yalitia hofu katika nyoyo za Mayahudi na wakawa na wasiwasi juu ya majumba yao zaidi.

4. *YESU ALIKAA MSALABANI SAA KIDOGO*

Miili ya watu waliopigiliwa msalabani siku ile. Yesu akiwa mmoja wao, iliondolewa baada ya muda mfupi usiotosha kumfanya mtu afe. Kwa ajili hii Pilato alistaajabu alipoambiwa kuwa Yesu amekwisha kufa (Marko 15:44), kwani alijua ya kuwa muda ule ulikuwa hautoshi kwa mtu kufa. Kadhalika wezi wawili waliokuwa wamepigiliwa siku ile pamoja na Yesu, walikuwa wazima wakati wote watatu wametolewa msalabani, na ikabidi miguu yao ivunjwe na wakauawa hivyo. Yesu alikuwa mtu mwenye afya sana, aliweza kukaa na njaa siku 40, usiku na mchana bila kula chakula (Matt. 4:2) asife, basi asingeweza kufa upesi namna hiyo mahali wengine hawakuweza kufa.

Kwa hekima ya Allah alikuwa amezimia, Askari waliowavunja wale wezi miguu, hawakumvunja Yesu, wakimdhani kafa. Inadhihirika ya kuwa akida aliyesimamia kusulubiwa kule, alikuwa na huruma juu ya Yesu, hata akafika kusema ya kuwa Yesu alikuwa mtu mwenye haki (Luka 23:47). Labda yeye aliwakataza askari wasimvunje Yesu miguu, kama walivyovunjwa wale wezi wawili. Ama mtu mzima kudhaniwa kafa si jambo la ajabu. Wasomao Injili

watakumbuka ya kwamba hata Paulo alipata kupigwa mawe na watu, wakimdhani kafa wakamkokotea nje ya mji. Baadae Paulo alipata fahamu (Matendo 14:19, 20).

5. *BISHARA ILITABIRI YESU ATAPONA*

Bishara iliyomo katika Zaburi 14:19-20 inaeleza ya kuwa Yesu ataponywa na maovu yote, na mifupa yake haitavunjwa. Hivyo kusema kuwa hakupona kifo cha msalaba, bali ikapona mifupa peke yake, ni dhahiri kucheza na bishara hiyo.

6. DAMU ILIKUWA IKITEMBEA

Askari mmoja alimchoma Yesu mkuki, "Ikatoka mara damu na maji" (Yohana 19:34). Hii ni alama inayojulikana sana ya uzima. Inaonyesha damu ilikuwa bado inatembea mwilini mwa Yesu. Damu haitoki "mara" katika mwili wa mtu aliyekwisha kufa.

7. KWA NINI YUSUFU ALIPEWA MWILI WA YESU?

Mara alifika mtu asiyekuwa jamaa ya Yesu, aitwaye Yusuf wa Arimathaya, mtu tajiri, na mfuasi wa Yesu kwa siri, akiwaogopa Mayahudi. Huyu aliomba kwa Pilato auchukue mwili wa Yesu (Yohana 19:38). Pilato alikubali tu bila kuuliza mwili huo umemhusu nini hali yeye si ndugu wa Yesu; kama ilivyokuwa desturi ya kuwa wanaouawa na serikali huwa hawachukuliwi ovyo, bali ni jamaa zao. Jambo hili linaonyesha kulikuwa mipango ya siri ya kumwokoa Yesu.

8. ULIKUWA MPANGO WA KUMWOKOA YESU

Yusuf wa Arimathaya pamoja na tabibu aitwaye Nikodemu waliuchukua mwili wa Yesu na wakaanza kuufanyia sawa na mipango waliyokwisha tayarisha. Hawakumpeleka kwenye makaburi wanayozikiwa watu wote. Bali walimlaza kwa uangalifu, si katika makaburi kama haya yetu ya kufukia kwa udongo, bali katika pango jipya lililokuwa kama chumba, lililochongwa na Yusuf katika mwamba wa jiwe, bustanini mwake. Lilikuwa na nafasi ya watu kadhaa kukaa salama ndani yake bila kukosa hewa. Kadhalika halikuwa na kifungio kilichosaki bila kuacha kengerezi za kupita hewa, bali lilikuwa na jiwe la mduwara lililochongwa vivyo hivyo tu kwa kuziba mlango wa pango hilo.

Sasa fikiri, tabibu yule aliletwa kwa haja gani? Pia ujuwe kuna dawa ya marahamu ambayo mpaka leo inajulikana katika vitabu vya utabibu kwa jina la marahamu ya Yesu. Dawa hiyo kali ilimponya Yesu majeraha ya msalabani. Usiku mzima wa Ijumaa ile na Jumamosi yake Yesu alifanyiwa kila namna ya juhudi kule faraghani pangoni, mpaka akapona kiasi cha kutosha. Wakati wote huo Mayahudi walikuwa wameshughulika na Sabato yao wasiwe na haja ya kufika huko. Siku ya Jumapili ambayo watu wengi wangeweza kufika kule pangoni na kutazama, alfajiri mapema Yesu alikuwa kishatolewa mle, asije akakutwa na kukamatwa tena.

9. MAYAHUDI WALIONA SHAKA JUU YA KUFA KWAKE

Mayahudi kutaka askari walinde pango alimotiwa Yesu, ni dalili inayoonyesha ya kwamba hawakuwa na yakini kuwa amekufa kabisa kabisa. Wangekuwa na hakika hiyo, ingewadhuru nini kama wafuasi wake wahamishe maiti yake? Sababu inayosemwa kwamba ili "wasije wanafunzi wake usiku wakamwiba, wakawaambia watu, amefufuka katika wafu" (Matt. 27:64), ni ya upuuzi, maana Mayahudi wangejibu, kama amefufuka, mtoeni aonekane na hapo wangeweza kumkamata tena.

10. *YESU ALIJIGEUZA ASIPATE KUKAMATWA TENA*

Mara baada ya kutoka pangoni, Yesu, alionekana na Mariamu katika mwili wake ule ule wa kibinadamu. Mariamu akamdhani ni mlinzi wa bustani (Yohana 20:15). Yumkini kwa sababu Yesu alijifananisha na mlinzi wa bustani. Inawezekana kabisa wale watu wawili waliokutwa na Mariamu ndani ya lile pango wamevaa mavazi meupe, ndio mlinda bustani wa Yusuf wa

Arimathaya na msaidizi wake, ambaye alimpatia Yesu nguo za kujibadili nazo. Na baadaye kwa sababu ya visa vya hadithi, hao watu wawili wakaanza kusemwa ni malaika, na wakazidi kutia chumvi kwa kusema mahali pengine kuwa ni malaika aliyeshuka mbinguni (Matt. 28:2). Wala mtu asione ajabu jiwe kufunguliwa mlangoni pa pango, maana waliolifunga hapo kwanza ndio waliolifungua kumtoa Yesu.

11. *YESU ALIOGOPA KUKAMATWA*

Yesu akawapelekea wafuasi wake ujumbe ya kuwa yeye anatangulia kwenda jimbo jingine la Galilaya, na ya kuwa waonane naye huko (Matt. 28:7), maana alijua ya kuwa Mayahudi punde watapata habari kuwa ameponyoka kufa pale msalabani, na wataanza kumsaka sana hadi kumpata.

12. *YESU HAKUPATA MWILI MPYA*

Yesu alijhadhari sana asionekane na Mayahudi. Watu aliokuwa akionana nao ni wanafunzi wake tu (Matendo 10:41), tena kwa siri, na hata hivyo hakuwa anakaa nao sana. Hakujionyesha kwa watu. Alikuwa ni mtu yule yule wa desturi, akiona njaa na kiu. Alipokutana na wanafunzi wake aliwaomba chakula, wakampa, akala mbele yao (Luka 20:42). Kadhalika aliwaambia wanafunzi wake ambao walimdhania kuwa pepo, "Tazameni mikono yangu, na miguu yangu, ya kuwa ni mimi mwenyewe. Nipapaseni, mkatazame: kwa maana pepo hana mwili na mifupa, kama mnionavyo mimi kuwa nayo" (Luka 24:39-40). Na pia akamwambia Tomas, aliyekuwa bado na shaka juu ya wanafunzi wengine kumwona Yesu, kuwa amguse ili naye ahakikishe mwenyewe kuwa yeye ndiye Yesu.

Yote haya yanaonyesha ya kuwa Yesu hakufa msalabani, alizimia tu pale, akadhaniwa amekufa, na rafiki zake na watu waliomhurumia walikuwa wamefanya mipango ya siri mbele, ya kumwokoa. Yanaonyesha ya kwamba Yesu alipotoka mle pangoni alikuwa na hali zote za kibinadamu, hakuwa na mwili wa kiroho unaoweza kusemwa kuwa na uwezo na wepesi wa kuogelea katika hewa. Kama mwili wa Yesu ulikuwa wa kiroho, je ule mwili wake wa kiutu ulikwenda wapi? Na kama Yesu hakusaidiwa na rafiki zake, ni wapi alipopata zile nguo alizovaa na kuonekana na Mariamu kama mtunza bustani? Alikuwa amevaa nguo, basi alizipata wapi? Nguo zake mwenyewe zilikuwa zimechukuliwa na askari, na sanda zilibaki katika lile pango la kaburi. Isitoshe Yusuf wa Arimathaya na Nikodemu, ambao ni watu waliochukua mwili wa Yesu toka mwanzo, wanaonekana wanafichwa, ili wasieleze habari zote zilizofanyika juu ya mwili wa Yesu uliokuwa mikononi mwao toka mwanzo. Hakuna mahali po pote katika Agano Jipya, panapoonyesha kuwa Yusuf wa Arimathaya na Nikodemu nao walisadiki kuwa Yesu amefufuka katika wafu. Hivyo hatuna njia ila kukataa kabisa shauri la kusema kuwa Yesu alikufa kifo cha laana cha msalabani. Hii ndiyo kweli ambayo imebainishwa na Qur'an kabla mtu ye yote hajafikiria jambo hili kwa kulitangaza; na leo wanazuoni wengi wa Kikristo pia wanalikubali.

13. *ISHARA YA KUKAA MZIMA*

Yesu mwenyewe alitabiri kuwa ataonyesha Ishara kama iliyoonyeshwa na Nabii Yunus zamani. Yesu alipoombwa kufanya Ishara alijibu: "Kizazi kibaya na cha zinaa chataka ishara, wala hakitapewa ishara, ila ishara ya Nabii Yunus. Maana kama vile Yunus alivyokuwa siku tatu mchana na usiku katika tumbo la nyangumi, hivyo ndivyo mwana wa Adamu atakavyokuwa siku tatu mchana na usiku katika moyo wa nchi" (Matt. 12:39-40).

Wakristo wanasadiki ya kuwa Yesu aliingia moyo wa nchi (yaani kaburi) hali amekufa, na baada ya mchana mmoja na mausiku mawili, akafufuka toka wafu. Lakini je, Nabii Yunus alionyesha Ishara ya kufufuka toka wafu? La. Kitabu chake kinatuambia ya kuwa aliingia tumboni mwa nyangumi hali yu mzima, akakaa humo hali yu mzima, na akatoka humo hali yu mzima. Hii ndiyo Ishara aliyobashiri Yesu, kuwa naye pia ataingia kaburini mzima, atakaa humo mzima, na atatoka mzima. Kama alikufa msalabani, basi hakuna Ishara yo yote tena. Maana Yesu hakuwa mle pangoni kwa siku tatu usiku na mchana, kama alivyokaa Yunus katika tumbo la nyangumi.

159. Bali Allah Alimnyanyua Kwake, na Allah ni Mwenye nguvu, Mwenye hekima.

بَلْ رَّفَعَهُ اللّٰهُ اِلَيْهِ ؕ وَكَانَ اللّٰهُ عَزِيْزًا حَكِيْمًا ﴿۱۵۹﴾

Bali alikaa humo kwa mausiku mawili na mchana mmoja. Hivyo hakuna kufanana hapa. Yunus aliingia tumboni mwa samaki. Yesu akaingia pango la jiwe. Hivi navyo ni tofauti. Jambo moja tu limebaki: ndio hali walizoingia nazo. Basi kama Yesu aliingia pangoni kafa, akakaa humo yu mfu, kisha akafufuka, hali yake haifanani hata kidogo na hali ya Yunus, aliyeingia mzima, akakaa humo mzima, na akatoka mzima. Kwa hiyo wanaosadiki kuwa Yesu alikufa msalabani, na kuingia kaburini kafa, wanaonyesha ya kuwa bishara iliyotolewa na Yesu haikutimia. Lakini matokeo yote ya habari za Yesu na msalaba tuliyokwisha yakagua huko juu yanaonyesha ya kuwa ishara hii ya Yesu ilitimia sawasawa, naye hakufa juu ya msalaba, bali alizimia tu, akadhaniwa kafa, baadaye rafiki zake wakamsaidia kwa kumtibu, na akasafiri kwa siri kuitoka nchi ya maadui zake. Wakristo na Mayahudi, kama isemavyo Qur'an, hawajui hakika ya jambo hili, isipokuwa wanafuata dhana tu.

Aya 159. *Allah Alimnyanyua Kwake.* Kwa maana ya neno rafa' "kunyanyua" tazama sura 2:64; 3:56. Mradi wa Aya hii ni kuwa Mayahudi walitaka waonyeshe kuwa kwa kufia msalabani, Nabii Isa ni mtu maluuni, na hana daraja yo yote kwa Allah. Allah hapa baada ya kueleza habari walizofanya Mayahudi, na jinsi Alivyopindua hila yao, anabainisha ya kuwa Nabii Isa si maluuni, bali ni mtu aliyenyanyuliwa kwa daraja mbele ya Allah kama Manabii wengine.

Tumekwisha soma katika maelezo ya juu fungu la 10, ya kuwa Yesu alipotoka ndani ya lile pango la kaburi alikuwa na mwili huu huu wa kibinadamu, alama za majeraha zilikuwa bado zingalipo, na alikula na akanywa. Aliogopa kujionyesha; na alikutana na wanafunzi wake peke yao, kwa kuogopa asikamatwe.

Angekuwa amefufuka toka wafu, au kama mwili wake ungekuwa si wa kibinadamu, asingeogopa kukamatwa na kuogopa kifo. Bali angejitoa kwa fahari mbele ya maadui zake na kuwaonyesha makarama yake na kutangaza kuwa ameshinda kifo. Zaidi ya hayo angeonyesha upendo wake kwa maadui zake kwa kuwahubiria ili wapate kumwamini kuwa ndiye Kristo wao, naye si mtu maluuni na mwongo kama walivyodhani. Kama Yesu alifufuka toka wafu, hayo yalikuwa ya lazima kabisa kufanya, na kuwatoa aibu wanafunzi wake, na Mayahudi wapate kumwamini. Lakini yeye hakufanya hivyo. Alijihadhari sana asionekane na kukamatwa.

1. *YESU HAKUWA NA MWILI MWEPESI*

Baadhi ya watu wanaelekea kudhani kuwa maneno haya, Ikawa jioni katika siku ile ya kwanza ya sabato, na milango imefungwa walipokuwepo wanafunzi kwa khofu ya Wayahudi, akaja Yesu, akasimama katikati, akawambia, Amani kwenu" (Yohana 20:9), yanaonyesha kwamba Yesu alikuwa na mwili wa kipepo. Lakini sivyo. Huko mbele tumekwisha soma, Yesu mwenyewe amekataa kuwa hana mwili wa kipepo. Jambo lenyewe si vigumu kufahamu lilivyokuwa. Nyumba ile ilikuwa ya marafiki za Yesu. Inawezekana Yesu alikuwemo katika nyumba ile amejificha kama desturi yake, kwa kuwaogopa Mayahudi, na wanafunzi wake walipokwisha kuwamo ndani, milango ya mbele ndio ikafungwa kwa hofu ya Mayahudi. Maneno hayo hayaonyeshi kuwa Yesu alipita pasipokuwa mlango. Basi ama alitoka katika chumba alimokuwa, na kuingia walikokuwa wafuasi wake au alikuwa mle mle chumbani kimya katika giza, kabla wao hawajaingia. Maelezo kama haya pia yameelezwa na Mr. Docker, mtungaji wa kitabu kiitwacho, "If Jesus did not die upon the Cross?" (kurasa 14-16).

2. *YESU HAKUPAA MBINGUNI*

Yesu amesema "Na hapana mtu aliyepanda mbinguni, ila yeye aliyeshuka kutoka mbinguni" (Yohana 3:13). Ni wazi ya kuwa Yesu hakushuka na mwili wa kibinadamu kutoka mbinguni, alizaliwa nao hapa duniani, na akakuzwa na vyakula na hewa na maji ya hapa duniani. Hivyo huu mwili wake usioshuka kutoka mbinguni asingeweza kupanda nao mbinguni, kwa mujibu wa maneno yake hayo. Hivyo, kusema ya kuwa Yesu mwenye mwili wa kidunia anakaa mkono wa kulia wa Mungu, ni fikira ya kipagani, na ya kichekesho, hata haihitaji hoja zaidi, maana tokeapo imekwisha batilika.

3. *INJILI YA MATHAYO HAISEMI ALIPAA*

Vifungu vya Agano Jipya vinavyoeleza habari za kupaa kwa Yesu havina utegememo wa kutosha kukubalisha jambo kubwa kama hili. Mattayo, ambaye anasemwa kuwa mwanafunzi hasa wa Yesu, hana habari hata kidogo kuwa Yesu alipaa. Haiwezekani asahau jambo hili kubwa kabisa la ajabu, tena la mwisho, na akumbuke mambo mengine madogo-madogo. Huyu Mathayo hana asemalo la mwisho wa Yesu ila hili tu ya kuwa, Yesu alipotoka katika lile pango la kaburi, alikwenda Galilaya na huko akakutana na wafuasi wake penye mlima aliowaambia, na huko akawapa maagizo fulani. Hivyo, juu ya shauri hili la kupanda Yesu mbinguni, mwanafunzi wake mmoja aliyekuwa shahidi amekwisha jitoa, anaonyesha kuwa yeye hajui habari hiyo!

4. *MANENO YALIONGEZWA KATIKA INJILI YA MARKO*

Marko, ambaye hakuwa mwanafunzi wa Yesu, wala hakushuhudia mkutano wa mwisho wa Yesu na wanafunzi wake, anatuambia ya kuwa Yesu alipeleka habari kwa wanafunzi wake akiwaambia wakutane naye Galilaya. Na bila kutaja walikutania wapi, mara anasema, "Basi Bwana, baada ya kusema nao, akachukuliwa juu mbinguni, akaketi mkono wa kuume wa Mungu" (Marko 16:19). Maneno yake ya mwisho, "Akaketi mkono wa kuume wa Mungu" yanadhoofisha kabisa habari yote, kwani haiyumkiniki ya kwamba aliyeandika hayo alifuatana na Yesu kwenda mwona akikaa, si mkono wa kushoto, bali mkono wa kulia wa Mungu.

Ukweli juu ya Aya za mwisho 12 za kitabu hiki cha Marko ni kwamba "ziliongezwa baadaye, yumkini mwanzoni mwa karne ya pili, yumkini kushika mahala pa maneno ya mwisho yaliyokuwa yamepotea, au yaliyoonekana yenye kasoro" (Encyclopaedia Britanica, Ed. 11 Vol. 17, p, 730). Hivyo maelezo ya Marko hayawezi kuchukuliwa kuwa msingi wa imani hii ya kupaa Yesu.

5. *LUKA HAKUMWONA AKIPAA*

Luka, ambaye pia hakuwa katika watu waliokuwa na Yesu alipoagana nao, na ambaye anakiri ya kuwa habari alizoandika yeye ni za kuhadithiwa na watu walioona (Luka 1:1). (ambao mmoja wa hao walioona, tumekwisha ona hana habari ya jambo hilo), ameandika hivi, "Akawaongoza nje mpaka Bethania: akainua mikono yake, akawabariki. Ikawa katika kuwabariki, akajitenga nao, akachukuliwa juu mbinguni" (Luka 24:50-51). Hivyo Luka anasema, Yesu alijitenga na wafuasi wake, ambayo ni maneno hayawezi kuleta maana ya kuwa wafuasi wake walimwona akipaa.

6. *YESU ALITEREMKA CHINI*

Tena tunasoma, "Akiisha kusema haya, walipokuwa wakitazama, aliinuliwa, wingu likampokea kutoka machoni pao" (Matendo 1:9). Sasa, kuondoka machoni pao, siyo maana yake kuwa alipaa. Inawezekana ya kwamba alipanda kwenye kilele cha mlima na kile kilele kilififizwa na mawingu au kungugu, wasiweze kumwona; kisha toka hapo akashuka upande wa pili wa mlima, akisafiri kwenda nchi nyingine atakakokuwa salama.

7. *YESU ALIHAMIA NCHI NYINGINE*

Yohana anasadikisha maneno haya kwa kusema ya kuwa Yesu mara ya mwisho alikutana na wafuasi wake kwenye bahari ya Tiberia, na akamwambia Petro "Lisha kondoo zangu"

160. Na hakuna ye yote katika watu wa Kitabu ila ataliamini kabla ya kifo chake, naye (Masihi) siku ya Kiyama atakuwa shahidi juu yao.

وَإِنْ مِّنْ أَهْلِ الْكِتٰبِ إِلَّا لَيُؤْمِنَنَّ بِهٖ قَبْلَ مَوْتِهٖ ۚ وَيَوْمَ الْقِيٰمَةِ يَكُوْنُ عَلَيْهِمْ شَهِيْدًا ﴿١٦٠﴾

(Yohana 21:17), na pia akasema, "Nifuate," na "Petro akigeuka, akamwona mwanafunzi yule aliyependwa na Yesu akifuata" (Yohana 21:19-20).

Hakuna shaka ya kwamba maneno haya ya Yohana yanaonyesha ya kwamba Yesu hakupanda mbinguni, bali alisafiri kwenda nchi nyingine. Ni dhahiri, basi, ya kuwa maandiko ya Mathayo na Yohana, ambao Wakristo wanawakubali kuwa wanafunzi halisi wa Yesu, hawajui kitu juu ya hii habari ya kupanda mbinguni, iliyosimuliwa ovyo ovyo na waandishi wengine waliokuja nyuma, bila ushahidi wo wote.

Maneno ya Marko yasemayo alipaa mbinguni si ya asili katika kitabu chake, bali yaliongezwa baadaye na mtu wasiyemjua.Luka anayesema juu juu habari za kupaa hakuwako pamoja na wanafunzi wa Yesu zama akiagana nao. Ushahidi zaidi unaotukataza kutegemea maneno yao ni kwamba wao wenyewe hawajasikilizana, na hawapatani katika mambo makubwa ya habari hii.

Mmoja anasema, Yesu alipaa alipokuwa Bethania (Luka 24:50-51). Mwingine anasema, Yesu alipaa alipokuwa mlima wa Mizeituni (Matendo 1:12). Tena mmoja anasema, alipaa siku aliyotoka katika kaburi au usiku uliofuata (Luka 24:21-29, 36 na 51). Lakini katika Matendo (1:3) tunasoma ya kuwa Yesu alipaa siku ya arobaini baada ya kufufuka wasemako. Mathayo anasema, Yesu alikwenda Galilaya, akaonana na wanafunzi wake huko; na Yohana anasema, aliagana na wanafunzi wake penye bahari ya Tiberia. Angalieni ni vurugu iliyoje hii!

8. *MAONI YA BWANA WEIGAL*

Mzungu mmoja, aitwaye Weigal ameandika:

"Kupaa hakutajwi katika maandiko ya kwanza ya Wakristo, yaani, Barua; wala haionekani kama kulitajwa katika Injili ya mwanzo kabisa ya Marko Mt. maana maneno haya "akachukuliwa juu mbinguni" si bayana kamwe, nayo ni katika Aya za mwisho kumi na mbili za kitabu hicho ambazo sasa zinakubaliwa na wanachuoni wa Biblia wote-wote ya kuwa ziliongezwa baadaye kabisa." Tena anasema: "Kupaa mbinguni kwa namna hii kulikuwa ni mwisho wa desturi wa hadithi za uwongo za miungu ya kipagani; kama ilivyokuwa kwa hadithi za uwongo za maisha ya Elijah. Mungu wa kipagani aitwaye Adonis, ambaye ibada yake ilistawi katika nchi ulimokulia Ukristo, alidhaniwa kupaa mbinguni mbele ya wafuasi wake baada ya kufufuka kwake; na kadhalika Dionysos, Herakles, Hyacinth, Krishna, Mithra, na miungu wengine walipaa mbinguni" (Weigal - Paganisim in our Christianity, pages 99, 100, 101).

Hivyo, mwisho wa maneno tunaoufikia ni kuwa, ni fujo kusimamisha habari za kupaa Yesu juu ya msingi ulio dhaifu namna hii.

Aya 160. Aya hii imekuwa chanzo cha mabishano kuhusu maana yake halisi. Baadhi ya wanazuoni wanaamini kwamba inazungumzia wakati ujao wa mbali kwa kulinganisha na wakati wa tukio la kusulubisha ikionyesha kwamba Mayahudi wote bila kuacha hata mmoja, siku moja watamwamini Yesu Kristo na kumkubali yeye kuwa ni Mtume wa kweli wa Allah. Wanadai kwamba imetajwa pia katika aya hii kuwa mwujiza huu ungetokea katika kipindi cha uhai wa Yesu Kristo. Wameongozwa kuwa na maoni haya kutokana na maneno *qabla mautihi* ambayo yanamaanisha kabla ya kifo chake.

Kwa kuwa Mayahudi bado hawajamkubali, kwa hiyo, kulingana na wanazuoni wa aina hiyo Yesu ni lazima awe bado yungali hai.

فَبِظُلْمٍ مِّنَ الَّذِيْنَ هَادُوْا حَرَّمْنَا عَلَيْهِمْ
طَيِّبٰتٍ اُحِلَّتْ لَهُمْ وَبِصَدِّهِمْ عَنْ سَبِيْلِ
اللّٰهِ كَثِيْرًا ﴿١٦١﴾

161. Basi wale waliokuwa Mayahudi, kutokana na dhulma yao na kutokana na kuizuia kwao mno njia ya Allah, basi Tukawaharamishia hata vile vitu vizuri walivyohalalishiwa (hapo kabla),

وَّاَخْذِهِمُ الرِّبٰوا وَقَدْ نُهُوْا عَنْهُ وَاَكْلِهِمْ
اَمْوَالَ النَّاسِ بِالْبَاطِلِ ؕ وَاَعْتَدْنَا
لِلْكٰفِرِيْنَ مِنْهُمْ عَذَابًا اَلِيْمًا ﴿١٦٢﴾

162. Na kwa sababu ya kuchukua kwao riba, hali wameikatazwa, na kula kwao mali za watu kwa batili. Na Tumewaandalia makafiri miongoni mwao adhabu iumizayo.

لٰكِنِ الرّٰسِخُوْنَ فِي الْعِلْمِ مِنْهُمْ
وَالْمُؤْمِنُوْنَ يُؤْمِنُوْنَ بِمَآ اُنْزِلَ اِلَيْكَ
وَمَآ اُنْزِلَ مِنْ قَبْلِكَ وَالْمُقِيْمِيْنَ الصَّلٰوةَ
وَالْمُؤْتُوْنَ الزَّكٰوةَ وَالْمُؤْمِنُوْنَ بِاللّٰهِ
وَالْيَوْمِ الْاٰخِرِ ؕ اُولٰٓئِكَ سَنُؤْتِيْهِمْ
اَجْرًا عَظِيْمًا ﴿١٦٣﴾ ع ٢٢

163. Lakini waliobobea ndani ya elimu miongoni mwao, na waaminio, wanaamini yaliyoteremshwa kwako na yaliyoteremshwa kabla yako, na wenye kusimamisha Sala na wanaotoa Zaka na wanaomwamini Allah na siku ya Mwisho. Hao ndio tutawapa malipo makubwa.

Maoni mengine yaliyoshikiliwa na watu wengi ni kwamba maneno *kabla ya kifo chake* yanamrejea kila mwanachama wa imani ya Kiyahudi wa zama za Yesu Kristo. Kwa ajili hiyo hii itakuwa na maana kwamba kila Myahudi atamwamini Yesu Kristo kabla ya kifo chake Myahudi huyo - dai linaloweza kuthibitishwa na Allah.

Kwa bahati mbaya matatizo na utatanishi mwingi vimesimama katika njia ya kuzikubali rai hizi moja kwa moja.

Sisi tunashauri ufumbuzi ambao ni tofauti na ni mpya kabisa juu ya tatizo hili. Aya hii inayochunguzwa inatafsiriwa hivi: 'Hakuna hata mtu mmoja miongoni mwa watu wa Kitabu ila bila shaka atamwamini kabla ya kifo chake'.

Neno mmoja halikutajwa kwa njia ya kuandikwa katika aya hii bali limedokezwa tu. Kama lingalitajwa basi aya hii ingesomeka kama ifuatavyo:

Wa in ahadun min ahlil Kitaabi.

Neno *ahadun* ndilo neno lililodokezwa. Tunashauri kwamba badala ya neno linalodokezwa kuwa *ahadun* tungelichukulia neno *fariiqun* kuwa ndio neno lidokezwalo. Kwa hali hiyo tafsiri ingepaswa kuwa hivi" Hakuna madhehebu au kundi lo lote kutoka katika watu wa Kitabu ila litamwamini yeye (Yesu Kristo) kabla ya kifo chake. Hili ni sharti ya kwamba Yesu Kriso ni lazima awe amehamia katika nchi zinazokaliwa na makabila yaliyopotea ya Waisraeli na katika kufanya hivyo alikamilisha kazi yake ya kufikisha ujumbe wake kwa mataifa yote kumi na mbili ya nyumba ya Israeli. Fikra hii inazidi kuungwa mkono kwa nguvu sana na utabiri wa Yesu Kristo ambamo amedai kwamba atakwenda kuwatafuta kondoo waliopotea wa nyumba ya Israeli. (Mathayo 15:24).

FUNGU 23

إِنَّآ أَوْحَيْنَآ إِلَيْكَ كَمَآ أَوْحَيْنَآ إِلَىٰ نُوحٍ
وَّالنَّبِيّٖنَ مِنۢ بَعْدِهٖ ۚ وَأَوْحَيْنَآ إِلَىٰٓ
إِبْرٰهِيمَ وَإِسْمٰعِيلَ وَإِسْحٰقَ وَيَعْقُوبَ
وَالْأَسْبَاطِ وَعِيسٰى وَأَيُّوبَ وَيُونُسَ
وَهٰرُونَ وَسُلَيْمٰنَ ۚ وَاٰتَيْنَا دَاوٗدَ زَبُورًا ﴿١٦٣﴾

164. Kwa yakini Tumekufunulia kama Tulivyomfunulia Nuhu na Manabii baada yake; na Tuliwafunulia Ibrahimu na Ismaili na Isihaka na Yakubu na wazao (wake), na Isa na Ayubu na Yunus na Harun na Suleimani; na Daudi Tukampa Zaburi.

وَرُسُلًا قَدْ قَصَصْنٰهُمْ عَلَيْكَ مِنْ قَبْلُ
وَرُسُلًا لَّمْ نَقْصُصْهُمْ عَلَيْكَ ۚ وَكَلَّمَ اللّٰهُ
مُوسٰى تَكْلِيمًا ﴿١٦٤﴾

165. Na (Tulituma) Mitume Tuliokuhadithia zamani; na Mitume ambao Hatukukuhadithia; na Allah Akasema sana na Musa.

رُسُلًا مُّبَشِّرِيْنَ وَمُنْذِرِيْنَ لِئَلَّا
يَكُوْنَ لِلنَّاسِ عَلَى اللّٰهِ حُجَّةٌۢ بَعْدَ الرُّسُلِ ۚ
وَكَانَ اللّٰهُ عَزِيْزًا حَكِيْمًا ﴿١٦٥﴾

166. Mitume, watoao habari nzuri na waonyao, ili watu wasiwe na hoja juu ya Allah baada ya Mitume; na Allah ni Mwenye nguvu, Mwenye hekima.

لٰكِنِ اللّٰهُ يَشْهَدُ بِمَآ أَنْزَلَ إِلَيْكَ أَنْزَلَهٗ
بِعِلْمِهٖ ۚ وَالْمَلٰٓئِكَةُ يَشْهَدُوْنَ ۚ وَكَفٰى بِاللّٰهِ
شَهِيْدًا ﴿١٦٦﴾

167. Lakini Allah Anayashuhudia Aliyokuteremshia, Ameyateremsha kwa elimu Yake, na Malaika pia wanashuhudia; na Allah Anatosha kuwa Shahidi.

إِنَّ الَّذِيْنَ كَفَرُوْا وَصَدُّوْا عَنْ سَبِيْلِ اللّٰهِ
قَدْ ضَلُّوْا ضَلٰلًا بَعِيْدًا ﴿١٦٧﴾

168. Hakika wale waliokufuru na kuzuilia (watu) njia ya Allah, bila shaka wamepotea upotevu wa mbali.

إِنَّ الَّذِيْنَ كَفَرُوْا وَظَلَمُوْا لَمْ يَكُنِ اللّٰهُ
لِيَغْفِرَ لَهُمْ وَلَا لِيَهْدِيَهُمْ طَرِيْقًا ﴿١٦٨﴾

169. Hakika wale waliokufuru na kudhulumu, haikuwa Allah Awasamehe wala Awaongoze njia,

إِلَّا طَرِيْقَ جَهَنَّمَ خٰلِدِيْنَ فِيْهَآ أَبَدًا ۚ
وَكَانَ ذٰلِكَ عَلَى اللّٰهِ يَسِيْرًا ﴿١٦٩﴾

170. Isipokuwa njia ya Jahannam, humo watakaa muda mrefu. Na hayo ni rahisi kwa Allah.

Aya 166. *Wasiwe na hoja juu ya Allah.* Allah anatuma Mitume Wake ili watu watakapoadhibiwa, wasipate hoja ya kusema kuwa, sisi tunaadhibiwa bure na hali hakuja mtu ye yote kutoka Kwako kutuonyesha njia na kututahadharisha na matokeo mabaya ya vitendo vyetu.

يٰٓاَيُّهَا النَّاسُ قَدْ جَآءَكُمُ الرَّسُوْلُ بِالْحَقِّ
مِنْ رَّبِّكُمْ فَاٰمِنُوْا خَيْرًا لَّكُمْ ؕ وَاِنْ
تَكْفُرُوْا فَاِنَّ لِلّٰهِ مَا فِى السَّمٰوٰتِ
وَالْاَرْضِ ؕ وَكَانَ اللّٰهُ عَلِيْمًا حَكِيْمًا ﴿۱۷۰﴾

171. Enyi watu, bila shaka amewafikieni Mtume kwa haki kutoka kwa Mola wenu, basi aminini, itakuwa bora kwenu. Na kama mtakataa, basi ni vya Allah vilivyomo mbinguni na ardhini; na Allah ni Mjuzi, Mwenye hekima.

يٰٓاَهْلَ الْكِتٰبِ لَا تَغْلُوْا فِىْ دِيْنِكُمْ وَلَا
تَقُوْلُوْا عَلَى اللّٰهِ اِلَّا الْحَقَّ ؕ اِنَّمَا الْمَسِيْحُ
عِيْسَى ابْنُ مَرْيَمَ رَسُوْلُ اللّٰهِ وَكَلِمَتُهٗ ۚ
اَلْقٰىهَآ اِلٰى مَرْيَمَ وَرُوْحٌ مِّنْهُ ۫ فَاٰمِنُوْا
بِاللّٰهِ وَرُسُلِهٖ ۚ وَلَا تَقُوْلُوْا ثَلٰثَةٌ ؕ اِنْتَهُوْا
خَيْرًا لَّكُمْ ؕ اِنَّمَا اللّٰهُ اِلٰهٌ وَّاحِدٌ ؕ سُبْحٰنَهٗٓ
اَنْ يَّكُوْنَ لَهٗ وَلَدٌ ۘ لَهٗ مَا فِى السَّمٰوٰتِ
وَمَا فِى الْاَرْضِ ؕ وَكَفٰى بِاللّٰهِ وَكِيْلًا ﴿۱۷۱﴾ ع ۲۳

172. Enyi watu wa Kitabu! msiruke mipaka ya dini yenu, wala msiseme juu ya Allah ila yaliyo kweli; Masihi Isa bin Mariamu ni Mtume wa Allah na neno Lake tu Alilompelekea Mariamu, na ni roho iliyotoka Kwake. Basi mwaminini Allah na Mitume Wake; wala msiseme watatu, jizuieni, itakuwa bora kwenu; bila shaka Allah ni Mungu Mmoja tu. Ni mbali na utakatifu Wake ya kwamba Awe na mwana. Ni vyake vilivyomo mbinguni na vilivyomo ardhini; na Allah Anatosha kuwa Mlinzi.

FUNGU 24

لَنْ يَّسْتَنْكِفَ الْمَسِيْحُ اَنْ يَّكُوْنَ عَبْدًا لِّلّٰهِ
وَلَا الْمَلٰٓئِكَةُ الْمُقَرَّبُوْنَ ؕ وَمَنْ يَّسْتَنْكِفْ
عَنْ عِبَادَتِهٖ وَيَسْتَكْبِرْ فَسَيَحْشُرُهُمْ اِلَيْهِ
جَمِيْعًا ﴿۱۷۲﴾

173. Masihi hatabeua kuwa mtumishi wa Allah wala Malaika waliokurubishwa; na atakayeibeua ibada Yake na kutakabari, basi hivi karibuni Atawakusanya wote Kwake.

Aya 172. *Kalimatuhuu,* "Neno Lake". Tazama sura 3:46.

Ruuhumminhu, "Roho iliyotoka Kwake." Maneno hayo yote mawili yametumiwa juu ya Nabii Isa kwa sababu Mayahudi walimkebehi yeye na mama yake. Maneno haya si kama yanampa cheo zaidi kuliko Mitume wengine bali yanamsafisha tu na lawama alizotiwa. Maneno haya yametumiwa katika Qur'an pia kwa ajili ya Mitume wengine na hata kwa ajili ya watu wasiokuwa Mitume kama Mariamu na watoto wa Adam (soma sura 58:23; 15:30; 32:10; na 21:29). Kadhalika neno *ruuh* (roho) maana yake ni: rehema, pumzi anazovuta mtu, wahyi au ufunuo, Qur'an, Malaika; na furaha (Lane).

فَاَمَّا الَّذِيْنَ اٰمَنُوْا وَعَمِلُوا الصّٰلِحٰتِ
فَيُوَفِّيْهِمْ اُجُوْرَهُمْ وَيَزِيْدُهُمْ مِّنْ
فَضْلِهٖ ۚ وَاَمَّا الَّذِيْنَ اسْتَنْكَفُوْا وَاسْتَكْبَرُوْا
فَيُعَذِّبُهُمْ عَذَابًا اَلِيْمًا ۙ وَّلَا يَجِدُوْنَ
لَهُمْ مِّنْ دُوْنِ اللّٰهِ وَلِيًّا وَّلَا نَصِيْرًا ﴿١٧٣﴾
يٰۤاَيُّهَا النَّاسُ قَدْ جَآءَكُمْ بُرْهَانٌ مِّنْ
رَّبِّكُمْ وَاَنْزَلْنَاۤ اِلَيْكُمْ نُوْرًا مُّبِيْنًا ﴿١٧٤﴾
فَاَمَّا الَّذِيْنَ اٰمَنُوْا بِاللّٰهِ وَاعْتَصَمُوْا بِهٖ
فَسَيُدْخِلُهُمْ فِيْ رَحْمَةٍ مِّنْهُ وَفَضْلٍ ۙ
وَّيَهْدِيْهِمْ اِلَيْهِ صِرَاطًا مُّسْتَقِيْمًا ؕ ﴿١٧٥﴾
يَسْتَفْتُوْنَكَ ؕ قُلِ اللّٰهُ يُفْتِيْكُمْ فِي الْكَلٰلَةِ ؕ
اِنِ امْرُؤٌا هَلَكَ لَيْسَ لَهٗ وَلَدٌ وَّلَهٗۤ
اُخْتٌ فَلَهَا نِصْفُ مَا تَرَكَ ۚ وَهُوَ
يَرِثُهَاۤ اِنْ لَّمْ يَكُنْ لَّهَا وَلَدٌ ؕ فَاِنْ كَانَتَا
اثْنَتَيْنِ فَلَهُمَا الثُّلُثٰنِ مِمَّا تَرَكَ ؕ
وَاِنْ كَانُوْۤا اِخْوَةً رِّجَالًا وَّنِسَآءً فَلِلذَّكَرِ
مِثْلُ حَظِّ الْاُنْثَيَيْنِ ؕ يُبَيِّنُ اللّٰهُ لَكُمْ
اَنْ تَضِلُّوْا ؕ وَاللّٰهُ بِكُلِّ شَيْءٍ عَلِيْمٌ ﴿١٧٦﴾ ع

174. Na ama wale walioamini na kufanya vitendo vizuri, basi Atawapa ujira wao sawasawa na kuwazidishia kwa fadhili Zake, lakini wale waliobeua na kufanya kiburi, basi Atawaadhibu kwa adhabu iumizayo, wala hawatapata rafiki wala msaidizi ye yote badala ya Allah.

175. Enyi watu bila shaka imewafikieni dalili kutoka kwa Mola wenu, na Tukawateremshieni nuru dhahiri.

176. Lakini, ama wale waliomwamini Allah na kumshika sawasawa, basi hao Atawaingiza katika rehema Zake na fadhili (Zake) na kuwaongoza Kwake kwa njia iliyonyooka.

177. Wanakuuliza, sema: Allah Anawapeni hukumu juu ya mkiwa. Kama mtu amekufa hali hana mtoto lakini anaye dada, basi kwake itakuwa nusu ya yale aliyoyaacha (Marehemu), na mtu huyu atamrithi (dada yake) ikiwa hana mwana. Na kama wao ni (madada) wawili, basi watapata thuluthi mbili za yale aliyoyaacha; na wakiwa ndugu wanaume na wanawake, basi mwanamume atapata sehemu sawa na ya wanawake wawili. Allah Anawabainishieni ili msipotee; Na Allah ni Mjuzi wa kila kitu.

Aya 175. *Dalili na Nuru dhahiri,* mradi wa haya maneno mawili ni Qur'an pamoja na Ishara zake na pia Mtume Muhammad *s.a.w.*

Aya 177. *Kalaala.* Tazama sura 4:13 na orodha uk. 189 - 190.
(Madada) wawili, hapa mradi wake ni madada wawili au zaidi ya wawili. Maana hii inaimarishwa na tendo la Mtume *s.a.w.* alipoitumia Aya hii wakati alipokufa Jabir na akaacha madada saba (Jarir, jalada 6, uk. 24).

Maelezo ya Aya 177 uk. 196

Orodha ya Warithi Pamoja na Sehemu Zao

(Orodha hii ni moja katika kurasa zote mbili. Toka kushoto mpaka kulia ni 1 mpaka 24)

Tumenakili orodha iliyotengenezwa na Maulana Abdur-Rahman Jatt, H.A., O.T., Mwalimu wa Elimu ya Mirathi na Fiq'ha katika Madrasa Ahmadiyya, Qadiani, kwa ajili ya wasomaji wa Tafsiri ya Qur'an. Orodha hii inajulisha ya kuwa mrithi au warithi katika hali mbalimbali wanapata sehemu gani katika mali iliyoachwa na maiti.

Nambari	Majina ya Warithi	*Kama hakuna mrithi mwingine*	*Kama kuna mtoto mmoja wa kiume au zaidi*	*Kama kuna binti*	*Kama kuna zaidi ya binti mmoja*	*Kama kuna mjukuu wa kiume mmoja au zaidi wa kuzaliwa na mtoto wa kiume*	*Kama kuna mjukuu wa kike aliyezaliwa na mtoto wa kiume*	*Kama kuna wajukuu wa kike waliozaliwa na mtoto wa kiume*	*kama kuna dada wa kwa baba na mama*	*Kama kuna madada wa kwa baba na mama.*
		1	2	3	4	5	6	7	8	9
1	Binti : Atapata	1/2	Asaba	2/3	2/3	1/2	1/2	1/2	1/2	1/2
2	Mabinti wawili au zaidi	2/3	Asaba	2/3	2/3	2/3	2/3	2/3	2/3	2/3
3	Mjukuu wa kike aliyezaliwa na mtoto wa kiume	1/2	x	1/6	x	Asaba	2/3	2/3	1/2	1/2
4	Wajukuu wa kike waliozaliwa na mtoto wa kiume	2/3	x	1/6	x	Asaba	2/3	2/3	2/3	2/3
5	Dada wa kwa baba na mama	1/2	x	Asaba	Asaba	x	Asaba	Asaba	2/3	2/3
6	Madada wa kwa baba na mama	2/3	x	Asaba	Asaba	x	Asaba	Asaba	2/3	2/3
7	Dada wa kwa baba tu	1/2	x	Asaba	Asaba	x	Asaba	Asaba	1/6	x
8	Madada wa kwa baba tu	2/3	x	Asaba	Asaba	x	Asaba	Asaba	1/6	x
9	Dada au ndugu wa kwa mama	1/6	x	x	x	x	x	x	1/6	1/6
10	Madada au ndugu zaidi wa kwa mama	1/2	x	x	x	x	x	x	1/3	1/3
11	Mama	1/3	1/6	1/6	1/6	1/6	1/6	1/6	1/3	1/6
12	Bibi wa kwa mama na mama ya bibi na mama ya mama ya bibi mpaka mwisho	1/6	1/6	1/6	1/6	1/6	1/6	1/6	1/6	1/6
13	Bibi wa kwa baba na mama ya bibi na mama ya mama ya bibi mpaka mwisho	1/6	1/6	1/6	1/6	1/6	1/6	1/6	1/6	1/6
14	Mke au wake	1/4	1/8	1/8	1/8	1/8	1/8	1/8	1/4	1/4
15	Mume	1/2	1/4	1/4	1/4	1/4	1/4	1/4	1/2	1/2
16	Baba	Asaba	1/6	1/6 + Asaba	1/6 + Asaba	1/6	1/6 + Asaba	1/6 + Asaba	Asaba	Asaba
17	Babu mzaa baba	Asaba	1/6	1/6 + Asaba	1/6 + Asaba	1/6	1/6 + Asaba	1/6 + Asaba	Asaba	Asaba
18	Mtoto au watoto wa kiume	Asaba	Asaba	Asaba	Asaba	Asaba	Asaba	Asaba	Asaba	Asaba
19	Mjukuu wa wajukuu wa kiume waliozaliwa na mtoto wa kiume	Asaba	x	Asaba	Asaba	Asaba	Asaba	Asaba	Asaba	Asaba
20	Ndugu wa kiume mmoja au zaidi wa kwa baba na mama	Asaba	x	Asaba	Asaba	x	Asaba	Asaba	Asaba	Asaba
21	Ndugu wa kiume mmoja au zaidi w a k w a b a b a	Asaba	x	Asaba	Asaba	x	Asaba	Asaba	Asaba * B x	Asaba * B x
u		Asaba	x	Asaba	Asaba	x	Asaba	Asaba	Asaba * B x	Asaba * B x

MAANA YA ALAMA ZILIZOTUMIWA KATIKA ORODHA HII

Neno Asaba katika Elimu ya Mirathi maana yake ni mrithi wa mali yote au wa mali yote inayobaki.

X Alama hii inaonyesha ya kuwa mrithi huyo pamoja na mrithi mwingine hatapata kitu. Kwa mfano, kama vile ndugu au baba hatakuwa na sehemu kukiwa mtoto.

- Alama hii inaonyesha kuwa warithi wa namna hii hawawi wawili.

thuluthi Baki. Yaani, mama atapata thuluthi ya mali iliyobaki baada ya kuwapa mke au mume.

1/6 + Asaba. Yaani, kwanza atapata kwa sababu yeye ni mrithi; na kama mali itabaki baada ya kuwapa Dhul-Faraaidh (yaani, wale ambao sehemu zao zimetajwa katika Qur'an), hiyo atapewa yeye.

* Alama hii inaonyesha kwamba kama dada awe Asaba, basi ndugu wa kwa baba wataanguka na hawatapewa cho chote. Na kama dada awe mrithi, basi ndugu hao watakuwa Asaba.

- x Asaba. Alama hii inaonyesha ya kuwa katika hali moja wataanguka, yaani hawatakuwa na fungu na katika hali nyingine watarithi kwa kuwa wao ni Asaba.

Kama kuna ndugu wa kiume wa kwa baba na mama	*Kama kuna ndugu za kiume wa kwa baba na mama*	*Kama kuna dada wa kwa baba tu*	*Kama kuna dada ziadi ya mmoja wa kwa baba tu*	*Kama kuna ndugu wa kwa baba tu*	*Kama kuna zaidi ya ndugu mmoja wa kwa baba tu*	*Kama kuna dada au ndugu wa kwa mama tu*	*Kama kuna madada au ndugu wa kwa mama tu*	*Kama kuna mama*	*Kama kuna bibi wa kwa baba*	*Kama kuna bibi wa kwa mama*	*Kama kuna mke au wake*	*Kama kuna mume*	*Kama kuna baba*	*Kama kuna babu mzaa baba.*
10	11	12	13	14	15	16	17	18	19	20	21	22	23	24
1/2	1/2	1/2	1/2	1/2	1/2	1/2	1/2	1/2	1/2	1/2	1/2	1/2	1/2	1/2
2/3	2/3	2/3	2/3	2/3	2/3	2/3	2/3	2/3	2/3	2/3	2/3	2/3	2/3	2/3
1/2	1/2	1/2	1/2	1/2	1/2	1/2	1/2	1/2	1/2	1/2	1/2	1/2	1/2	1/2
2/3	2/3	2/3	2/3	2/3	2/3	2/3	2/3	2/3	2/3	2/3	2/3	2/3	2/3	2/3
Asaba	Asaba	1/2	1/2	1/2	1/2	1/2	1/2	1/2	1/2	1/2	1/2	1/2	x	x
2/3	2/3	2/3	2/3	2/3	2/3	2/3	2/3	2/3	2/3	2/3	2/3	2/3	x	x
x	x	2/3	2/3	Asaba	Asaba	1/2	1/2	1/2	1/2	1/2	1/2	1/2	x	x
x	x	2/3	2/3	Asaba	Asaba	2/3	2/3	2/3	2/3	2/3	2/3	2/3	x	x
1/6	1/6	1/6	1/6	1/6	1/6	1/3	1/3	1/6	1/6	1/6	1/6	1/6	x	x
1/3	1/3	1/3	1/3	1/3	1/3	1/3	1/3	1/3	1/3	1/3	1/3	1/3	x	x
1/3	1/6	1/3	1/6	1/3	1/6	1/3	1/6	-	1/3	1/3	Thu-luthi Baki	Thu-luthi Baki	1/3	1/3
1/6	1/6	1/6	1/6	1/6	1/6	1/6	1/6	x	1/6	1/6	1/6	1/6 1/6	1/6	1/6
1/6	1/6	1/6	1/6	1/6	1/6	1/6	1/6	x	1/6	1/6	1/6	1/6	x	1/6
1/4	1/4	1/4	1/4	1/41/4	1/4	1/4	1/4	1/4	1/4	1/4	1/4	-	1/4	1/4
1/2	1/2	1/2	1/2	1/2	1/2	1/2	1/2	1/2	1/2	1/2	1/2	-	1/2	1/2
Asaba	Asaba	Asaba	Asaba	Asaba	Asaba	Asaba	Asaba	Asaba	Asaba	Asaba	Asaba	Asaba	-	Asaba
Asaba	Asaba	Asaba	Asaba	Asaba	Asaba	Asaba	Asaba	Asaba	Asaba	Asaba	Asaba	Asaba	x	-
Asaba	Asaba	Asaba	Asaba	Asaba	Asaba	Asaba	Asaba	Asaba	Asaba	Asaba	Asaba	Asaba	Asaba	Asaba
Asaba	Asaba	Asaba	Asaba	Asaba	Asaba	Asaba	Asaba	Asaba	Asaba	Asaba	Asaba	Asaba	Asaba	Asaba
Asaba	Asaba	Asaba	Asaba	Asaba	Asaba	Asaba	Asaba	Asaba	Asaba	Asaba	Asaba	Asaba	x	x
x	x	Asaba	Asaba	Asaba	Asaba	Asaba	Asaba	Asaba	Asaba	Asaba	Asaba	Asaba	x	x
x	x	Asaba * B x	Asaba * B x	x	x	Asaba	Asaba	Asaba	Asaba	Asaba	Asaba	Asaba	x	x

سُوْرَةُ الْمَآئِدَةِ مَدَنِيَّةٌ وَّ هِيَ مَعَ الْبَسْمَلَةِ مِائَةٌ وَّاِحْدٰى وَ عِشْرُوْنَ اٰيَةً وَّ سِتَّةَ عَشَرَ رُكُوْعًا

5. SURA AL-MAAIDA

Imeteremshwa Madina

Ina mafungu 16 na Aya 121 pamoja na Bismillahi

بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ ①

1. Kwa jina la Allah, Mwingi wa rehema, Mwingi wa ukarimu.

يٰۤاَيُّهَا الَّذِيْنَ اٰمَنُوْۤا اَوْفُوْا بِالْعُقُوْدِ ؕ اُحِلَّتْ لَكُمْ بَهِيْمَةُ الْاَنْعَامِ اِلَّا مَا يُتْلٰى عَلَيْكُمْ غَيْرَ مُحِلِّى الصَّيْدِ وَاَنْتُمْ حُرُمٌ ؕ اِنَّ اللّٰهَ يَحْكُمُ مَا يُرِيْدُ ②

2. Enyi mlioamini tekelezeni wajibu (wenu). Mmehalalishiwa wanyama wenye miguu minne, ila wale mnaosomewa, bila kuhalalisha mawindo mkiwa katika Haji. Allah Anahukumu Apendavyo.

يٰۤاَيُّهَا الَّذِيْنَ اٰمَنُوْا لَا تُحِلُّوْا شَعَآئِرَ اللّٰهِ وَلَا الشَّهْرَ الْحَرَامَ وَلَا الْهَدْىَ وَلَا الْقَلَآئِدَ وَلَاۤ آٰمِّيْنَ الْبَيْتَ الْحَرَامَ يَبْتَغُوْنَ فَضْلًا مِّنْ رَّبِّهِمْ وَ رِضْوَانًا ؕ وَ اِذَا حَلَلْتُمْ فَاصْطَادُوْا ؕ وَلَا يَجْرِمَنَّكُمْ شَنَاٰنُ

3. Enyi mlioamini! msivunje heshima ya alama za Allah, wala ya mwezi uliotukuzwa, wala ya dhabihu, wala ya makoja (yao), wala ya wale wakusudiao kwenda kwenye nyumba takatifu kutafuta fadhili za Mola wao na radhi (Yake). Na mtokapo katika Ihramu, basi windeni. Na uadui wa watu

---

Sura hii imepata jina lake katika dua ambayo Nabii Isa aliombwa na wanafunzi wake aiombe kwa ajili ya mafanikio ya kidunia ya dini ya Kikristo, ambayo yanaelezwa katika Aya 113-116 za sura hii.

Wafasiri mbalimbali wanasema ya kuwa sura hii ilishuka Madina. Hakim na Imam Ahmad wanasema ya kuwa Bibi Aisha alisema kwamba hii ni sura ya mwisho iliyoteremshwa kwa Mtume *s.a.w.* Tunapozifikiria pamoja hadithi zote, inaonekana ya kwamba bila shaka sura hii iliteremshwa katika miaka ya mwisho ya ujumbe wa Mtume *s.a.w.* Na ingawa Imam Ahmad anasema kwa ushahidi wa Asma binti Yazid ya kuwa sura hii yote ilishuka mara moja, lakini inaonekana ya kwamba sehemu yake kubwa ilishuka wakati mmoja, na kwahiyo ikaonekana kwamba yote ilishuka wakati mmoja. Neno Al-Maaida maana yake ni "Chakula" au *"Meza iliyopangwa chakula".*

Aya 2. *'Uquud,* "Wajibu," lina maana hizi: mapatano, maagano, ahadi, sharti, madaraka, mikataba, kanuni za Mungu (Lane na Akrab).

Aya 3. *Alama za Allah* ni kitu cho chote kinachowezesha kumjua Allah. Vitu vilivyotakaswa vyaweza kujumuisha vipindi fulani fulani vya wakati, mwahali au viumbe hai. Kafara zinazotolewa kwa ajili ya Mungu na wanyama wanaoletwa kwenye Kaaba kwa ajili ya dhabihu ni "Alama za Allah" kwa maana ya kuwa zinatufundisha tuwe tayari kila siku kutoa sadaka vitu vyetu kwa ajili ya Allah.

قَوْمٍ اَنْ صَدُّوْكُمْ عَنِ الْمَسْجِدِ الْحَرَامِ اَنْ
تَعْتَدُوْا ۘ وَتَعَاوَنُوْا عَلَى الْبِرِّ وَالتَّقْوٰى ۖ
وَلَا تَعَاوَنُوْا عَلَى الْاِثْمِ وَالْعُدْوَانِ ۖ
وَاتَّقُوا اللّٰهَ ؕ اِنَّ اللّٰهَ شَدِيْدُ الْعِقَابِ ۝٣

usiwashawishini kwa sababu waliwazuilieni Msikiti uliotukuzwa, ya kwamba mruke mipaka. Na saidianeni katika wema na utawa, wala msisaidiane katika dhambi na uasi. Na mcheni Allah; hakika Allah ni mkali wa kuadhibu.

حُرِّمَتْ عَلَيْكُمُ الْمَيْتَةُ وَالدَّمُ وَلَحْمُ
الْخِنْزِيْرِ وَمَآ اُهِلَّ لِغَيْرِ اللّٰهِ بِهٖ
وَالْمُنْخَنِقَةُ وَالْمَوْقُوْذَةُ وَالْمُتَرَدِّيَةُ
وَالنَّطِيْحَةُ وَمَآ اَكَلَ السَّبُعُ اِلَّا مَا ذَكَّيْتُمْ ۖ
وَمَا ذُبِحَ عَلَى النُّصُبِ وَاَنْ تَسْتَقْسِمُوْا
بِالْاَزْلَامِ ؕ ذٰلِكُمْ فِسْقٌ ؕ اَلْيَوْمَ يَئِسَ
الَّذِيْنَ كَفَرُوْا مِنْ دِيْنِكُمْ فَلَا تَخْشَوْهُمْ
وَاخْشَوْنِ ؕ اَلْيَوْمَ اَكْمَلْتُ لَكُمْ دِيْنَكُمْ
وَاَتْمَمْتُ عَلَيْكُمْ نِعْمَتِيْ وَرَضِيْتُ
لَكُمُ الْاِسْلَامَ دِيْنًا ؕ فَمَنِ اضْطُرَّ فِيْ
مَخْمَصَةٍ غَيْرَ مُتَجَانِفٍ لِّاِثْمٍ ۙ فَاِنَّ اللّٰهَ
غَفُوْرٌ رَّحِيْمٌ ۝٤

4. Mmeharamishiwa nyamafu na damu na nyama ya nguruwe, na kilicho-somewa jina lisilo la Allah, na kilichonyongwa, na kilichokufa kwa kupigwa, na kilichokufa kwa kuanguka, na kilichokufa kwa kupigwa pembe, na alichokula mnyama mkali, isipokuwa mlichochinja (kwa sheria), na (pia mmeharimishiwa) kilichochinjwa juu ya mawe ya sanamu, na (ni haramu kwenu) kugawanya kwa mishale ya kuagua. Hayo ni uasi. Leo wale waliokufuru wamekata tamaa katika dini yenu, basi msiwaogope, bali Niogopeni Mimi. Leo Nimewakamilishieni dini yenu, na kuwatimizieni neema Yangu, na Nimewapendeleeni Islamu iwe dini yenu. Lakini mwenye kushurutishwa na njaa, pasipo kuelekea kwenye dhambi, basi hakika Allah ni Msamehevu, Mrehemevu.

Mwezi uliotukuzwa, mradi wake ni kila mwezi katika miezi minne mitukufu: *Shawwaal, Dhul-Qaada, Dhul-Hijja,* na *Rajab.* Lakini baadhi ya maulamaa wanasema ya kuwa hapa *mwezi uliotukuzwa ni Dhul-Hijja* tu, yaani mwezi wa Haji Kubwa. Maulamaa wengine wanasema *mwezi uliotukuzwa* hapa ni mwezi wa *Rajab,* ambao ni mwezi wa Haji Ndogo na uliokuwa hauheshimiwi na baadhi ya makabila ya Waarabu.

Aya 4. *Leo Nimewakamilishieni dini yenu.* Aya hii ndiyo ya mwisho kuteremshwa kama wanavyokubaliana wanazuoni wote, na baada yake Mtume s.a.w. aliishi siku 82 tu akafariki (Razi).

Tangazo hili la Allah ni lenye maana sana. Qur'an ni sheria ya kwanza na ya mwisho inayodai kuwa kamilifu. Vitabu vya zamani havingeweza kusema hayo kwa kuwa vilikusudiwa kwa mataifa fulani na wakati maalumu. Taurati na Injili vilikuwa na nuru na mwongozo (sura 5:45, 47), lakini vikachanganywa na maneno ya watu vikatanguliwa na Qur'an.

يَسْـَٔلُوْنَكَ مَاذَآ اُحِلَّ لَهُمْ ؕ قُلْ اُحِلَّ لَكُمُ
الطَّيِّبٰتُ ۙ وَمَا عَلَّمْتُمْ مِّنَ الْجَوَارِحِ
مُكَلِّبِيْنَ تُعَلِّمُوْنَهُنَّ مِمَّا عَلَّمَكُمُ اللّٰهُ ۫
فَكُلُوْا مِمَّآ اَمْسَكْنَ عَلَيْكُمْ وَاذْكُرُوا
اسْمَ اللّٰهِ عَلَيْهِ ۠ وَاتَّقُوا اللّٰهَ ؕ اِنَّ اللّٰهَ
سَرِيْعُ الْحِسَابِ ۝٥

5. Wanakuuliza wamehalalishiwa nini, Sema: Mmehalalishiwa vitu vizuri, na mlichowafundisha wanyama wa kuwindia, kwa kuwafunza kuwinda- mnawafundisha Alivyowafunzeni Allah. Basi kuleni walichowakamatieni, na mkisomee jina la Allah; Na Mwogopeni Allah; hakika Allah ni Mwepesi wa kuhesabu.

اَلْيَوْمَ اُحِلَّ لَكُمُ الطَّيِّبٰتُ ؕ وَطَعَامُ
الَّذِيْنَ اُوْتُوا الْكِتٰبَ حِلٌّ لَّكُمْ ۖ
وَطَعَامُكُمْ حِلٌّ لَّهُمْ ۫ وَالْمُحْصَنٰتُ مِنَ
الْمُؤْمِنٰتِ وَالْمُحْصَنٰتُ مِنَ الَّذِيْنَ اُوْتُوا
الْكِتٰبَ مِنْ قَبْلِكُمْ اِذَآ اٰتَيْتُمُوْهُنَّ
اُجُوْرَهُنَّ مُحْصِنِيْنَ غَيْرَ مُسٰفِحِيْنَ
وَلَا مُتَّخِذِيْٓ اَخْدَانٍ ؕ وَمَنْ يَّكْفُرْ
بِالْاِيْمَانِ فَقَدْ حَبِطَ عَمَلُهٗ ۫ وَهُوَ فِى
الْاٰخِرَةِ مِنَ الْخٰسِرِيْنَ ۝٦ ع ١

6. Leo mmehalalishiwa vitu vizuri. Na chakula cha wale waliopewa Kitabu ni halali kwenu, na chakula chenu ni halali kwao. Na wanawake wema katika waaminio na wanawake wema katika wale waliopewa Kitabu kabla yenu (ni halali kwenu), mtakapowapa mahari zao, mkifunga nao ndoa, bila kufanya uzinzi, wala msiweke mahawara wa siri. Na anayekataa imani, bila shaka amali yake imepotea, na yeye katika Akhera atakuwa miongoni mwa wenye hasara.

Injili yenyewe inaahidi kufika kwa Mtume mwingine ambaye atawaongoza watu kwenye haki yote (Yohana 16:12-13).

Neno jingine la kukumbuka ni hili, kusema kuwa dini imekamilika siyo maana yake kuwa na watu pia wamekamilika na hawawezi kuharibika. Hivyo ukamilifu wa Islam umejaalia kuwa mara kwa mara wafike watu wa Mungu ili kuwaongoza Waislamu. Kwa ajili hii Mtume s.a.w. alisema; "Allah ataleta mwanzo wa kila miaka mia mtu wa kutilia nguvu dini." (Dawud, sura *Malaahim*).

Aya 5. *Wanyama na ndege wa mawindo.* Wanyama na ndege wanaokusudiwa kuwinda wanaweza kufugwa. Mtume *s.a.w.* alisema, wanyama na ndege hao watumwe kwa jina la Allah, nao wakiua mnyama au ndege aliye halali inajuzu kula. Lakini mawindo yakiletwa basi yachinjwe kama desturi ya Kiislamu (Muslim).

Watu wasio na ujuzi mwingi wa mafundisho ya Kiislamu wanafikiri kwamba kufuga mbwa kumekatazwa. Fikira hiyo haina ukweli. Mnyama yo yote awindaye anaweza kufugwa na kufundishwa kuwinda. Lakini ikumbukwe ya kuwa wanyama hao ni najisi, wasiruhusiwe kutangatanga ovyo nyumbani, ili wasipate kunusa vyombo na kuchafua vitu. Mbwa huwa na vijidudu vibaya vya maradhi, inafaa kujihadhari sana nao. Mbwa wanaponusa chombo au kukilamba, basi kikoshwe kwa mchanga na kwa maji kabla hakijatumiwa.

Aya 6. Aya hii inaeleza kuwa kama mtu katika watu wa Kitabu atamkaribisha Mwislamu

FUNGU 2

يٰٓاَيُّهَا الَّذِيْنَ اٰمَنُوْٓا اِذَا قُمْتُمْ اِلَى الصَّلٰوةِ
فَاغْسِلُوْا وُجُوْهَكُمْ وَاَيْدِيَكُمْ اِلَى
الْمَرَافِقِ وَامْسَحُوْا بِرُءُوْسِكُمْ
وَاَرْجُلَكُمْ اِلَى الْكَعْبَيْنِ ؕ وَاِنْ كُنْتُمْ
جُنُبًا فَاطَّهَّرُوْا ؕ وَاِنْ كُنْتُمْ مَّرْضٰٓى اَوْ
عَلٰى سَفَرٍ اَوْ جَآءَ اَحَدٌ مِّنْكُمْ مِّنَ الْغَآئِطِ
اَوْ لٰمَسْتُمُ النِّسَآءَ فَلَمْ تَجِدُوْا مَآءً
فَتَيَمَّمُوْا صَعِيْدًا طَيِّبًا فَامْسَحُوْا
بِوُجُوْهِكُمْ وَاَيْدِيْكُمْ مِّنْهُ ؕ مَا يُرِيْدُ
اللّٰهُ لِيَجْعَلَ عَلَيْكُمْ مِّنْ حَرَجٍ وَّلٰكِنْ
يُّرِيْدُ لِيُطَهِّرَكُمْ وَلِيُتِمَّ نِعْمَتَهٗ
عَلَيْكُمْ لَعَلَّكُمْ تَشْكُرُوْنَ ۝٧

7. Enyi mlioamini! mnaposimama kwa Sala, basi osheni nyuso zenu, na mikono yenu mpaka viwikoni, na mpake vichwa vyenu, na (osheni) miguu yenu mpaka vifundoni. Na mkiwa na janaba, basi ogeni. Na mkiwa wagonjwa au safarini, au mmoja wenu ametoka chooni au mmeingiliana na wanawake, na hamkupata maji, basi tayamamuni udongo ulio safi na kuupaka nyuso zenu na mikono yenu. Hapendi Allah kuwatieni katika taabu, bali Hutaka kuwatakaseni na kutimiza neema Yake juu yenu, ili mpate kushukuru.

وَاذْكُرُوْا نِعْمَةَ اللّٰهِ عَلَيْكُمْ وَمِيْثَاقَهُ
الَّذِيْ وَاثَقَكُمْ بِهٖٓ ۙ اِذْ قُلْتُمْ سَمِعْنَا
وَاَطَعْنَا ۡ وَاتَّقُوا اللّٰهَ ؕ اِنَّ اللّٰهَ عَلِيْمٌۢ بِذَاتِ
الصُّدُوْرِ ۝٨

8. Na kumbukeni neema ya Allah iliyo juu yenu, na ahadi Yake Aliyofungamana nanyi, mliposema: Tumesikia na tumetii. Na Mwogopeni Allah. Hakika Allah Hujua yaliyomo vifuani.

يٰٓاَيُّهَا الَّذِيْنَ اٰمَنُوْا كُوْنُوْا قَوّٰمِيْنَ لِلّٰهِ
شُهَدَآءَ بِالْقِسْطِ ۡ وَلَا يَجْرِمَنَّكُمْ شَنَاٰنُ
قَوْمٍ عَلٰٓى اَلَّا تَعْدِلُوْا ؕ اِعْدِلُوْا ۟ هُوَ
اَقْرَبُ لِلتَّقْوٰى ۡ وَاتَّقُوا اللّٰهَ ؕ اِنَّ اللّٰهَ
خَبِيْرٌۢ بِمَا تَعْمَلُوْنَ ۝٩

9. Enyi mlioamini! kuweni wasimamizi kwa ajili ya Allah, mtoao shahada kwa uadilifu. Na uadui wa watu usiwashawishini ya kwamba msifanye uadilifu. Fanyeni uadilifu, huo ni karibu sana na utawa, na Mcheni Allah. Hakika Allah Anazo habari za yale mnayoyatenda

kwenye chakula, Mwislamu anayo ruhusa kula, kwa sharti kuwa vyakula vyenyewe visiwe vilivyoharimishwa na dini ya Kiislamu. Kadhalika Mwislamu anayo ruhusa kuwakaribisha watu wa Kitabu katika chakula.

Na maneno haya, *Na wanawake wema katika waaminio na wanawake wema katika wale waliopewa Kitabu kabla yenu (ni halali kwenu),* yanakusudia kudokeza ya kwamba ingawa Islam inaruhusu Waislamu wanaume kuwaoa wanawake wasiokuwa Waislamu miongoni mwa watu wa Kitabu, lakini inapendelea zaidi wanaume wa Kiislamu kwa desturi wawaoe wanawake wa Kiislamu tu.

Aya 9. Kwa hakika hakuna dini nyingine inayotoa mafundusho ya haki namna hii kwa ajili ya maadui zao. Muislamu wa kweli awatendee kwa haki, siyo Waislamu tu, bali pia wasio Waislamu, na hata wale walio maadui zake.

وَعَدَ اللّٰهُ الَّذِيْنَ اٰمَنُوْا وَعَمِلُوا الصّٰلِحٰتِ ۙ لَهُمْ مَّغْفِرَةٌ وَّ اَجْرٌ عَظِيْمٌ ۝١٠

10. Allah Amewaahidi wale walioamini na kufanya vitendo vizuri (ya kwamba) watapata msamaha na malipo makubwa.

وَالَّذِيْنَ كَفَرُوْا وَكَذَّبُوْا بِاٰيٰتِنَآ اُولٰٓئِكَ اَصْحٰبُ الْجَحِيْمِ ۝١١

11. Na wale waliokufuru na kuzikadhibisha Aya Zetu, hao ndio watu wa Motoni.

يٰٓاَيُّهَا الَّذِيْنَ اٰمَنُوا اذْكُرُوْا نِعْمَتَ اللّٰهِ عَلَيْكُمْ اِذْ هَمَّ قَوْمٌ اَنْ يَّبْسُطُوْٓا اِلَيْكُمْ اَيْدِيَهُمْ فَكَفَّ اَيْدِيَهُمْ عَنْكُمْ ۚ وَاتَّقُوا اللّٰهَ ؕ وَعَلَى اللّٰهِ فَلْيَتَوَكَّلِ الْمُؤْمِنُوْنَ ۝١٢

12. Enyi mlioamini! kumbukeni neema za Allah zilizo juu yenu waliponuia watu kuwanyoosheeni mikono yao, lakini yeye Akaizuia mikono yao kufika kwenu; na muogopeni Allah. Na waaminio wamtegemee Allah.

FUNGU 3

وَلَقَدْ اَخَذَ اللّٰهُ مِيْثَاقَ بَنِيْٓ اِسْرَآءِيْلَ ۚ وَبَعَثْنَا مِنْهُمُ اثْنَيْ عَشَرَ نَقِيْبًا ؕ وَقَالَ اللّٰهُ اِنِّيْ مَعَكُمْ ؕ لَئِنْ اَقَمْتُمُ الصَّلٰوةَ وَاٰتَيْتُمُ الزَّكٰوةَ وَاٰمَنْتُمْ بِرُسُلِيْ وَعَزَّرْتُمُوْهُمْ وَاَقْرَضْتُمُ اللّٰهَ قَرْضًا حَسَنًا لَّاُكَفِّرَنَّ عَنْكُمْ سَيِّاٰتِكُمْ وَلَاُدْخِلَنَّكُمْ جَنّٰتٍ تَجْرِيْ مِنْ تَحْتِهَا الْاَنْهٰرُ ۚ فَمَنْ كَفَرَ بَعْدَ ذٰلِكَ مِنْكُمْ فَقَدْ ضَلَّ سَوَآءَ السَّبِيْلِ ۝١٣

13. Na bila shaka Allah alifunga ahadi na wana wa Israeli; na Tukainua miongoni mwao masultani kumi na mbili. Na Allah Akasema: Kwa yakini Mimi ni pamoja nanyi kama mkisimamisha Sala na mkitoa Zaka na mkiwaamini Mitume Wangu na kuwasaidia na kumpa Allah karadha iliyo nzuri, bila shaka Nitawafutieni maovu yenu na kuwaingizeni katika Mabustani yapitayo mito ndani yake. Lakini atakayekataa baada ya hayo miongoni mwenu, bila shaka amepotea njia iliyo sawa.

Aya 13. *Masultani kumi na mbili.* Pengine imesemwa ni Manabii kumi na mbili waliokuja baada ya Nabii Musa.

Pengine hakuna neno moja liwezalo kulitafsiri vya kutosha neno *naqiiba*. Halina maana ya kiongozi tu bali pia lina maana ya mtangazaji, yule ambaye anayo mamlaka ya kulisoma tangazo au kutoa hukumu kwa niaba ya mkuu wa nchi au watu wengine wenye mamlaka ya juu.

Karadha iliyo nzuri, mradi wake ni matendo mazuri yatakayoleta malipo mema kutoka kwa Allah, au mradi wake ni mchango unaotolewa kwa hiari kusaidia dini. Maneno haya wanaambiwa Waisraeli

فَبِمَا نَقْضِهِمْ مِّيْثَاقَهُمْ لَعَنّٰهُمْ وَجَعَلْنَا
قُلُوْبَهُمْ قٰسِيَةً ۚ يُحَرِّفُوْنَ الْكَلِمَ عَنْ
مَّوَاضِعِهٖ ۙ وَنَسُوْا حَظًّا مِّمَّا ذُكِّرُوْا بِهٖ ۚ
وَلَا تَزَالُ تَطَّلِعُ عَلٰى خَآئِنَةٍ مِّنْهُمْ اِلَّا
قَلِيْلًا مِّنْهُمْ فَاعْفُ عَنْهُمْ وَاصْفَحْ ؕ اِنَّ
اللّٰهَ يُحِبُّ الْمُحْسِنِيْنَ ⑬

14. Na kwa sababu ya kuvunja kwao ahadi yao, Tumewalaani na Tumeifanya mioyo yao kuwa migumu. Huyabadilisha maneno toka mahali pao, na kusahau sehemu ya yale waliyokumbushwa. Na utaendelea kupata habari za hiana yao, isipokuwa wachache miongoni mwao. Basi wasamehe na onyesha uvumilivu; hakika Allah Huwapenda wafanyao hisani.

وَمِنَ الَّذِيْنَ قَالُوْٓا اِنَّا نَصٰرٰٓى اَخَذْنَا
مِيْثَاقَهُمْ فَنَسُوْا حَظًّا مِّمَّا ذُكِّرُوْا بِهٖ ۠

15. Na kwa wale waliosema, Hakika sisi ni Wakristo, Tulishika ahadi yao,

---

Aya 14. *Huyabadilisha maneno toka mahali pao.* Kuharibika kwa Vitabu vya Wakristo ni jambo ambalo linakubaliwa na wanazuoni wakubwa wakubwa wa Ulaya. Wao wameandika maneno ambayo tunayanakili hapa:-

1. "Tukigeukia kwenye historia ya ndani ya maandiko ya Agano Jipya, ni wazi ya kuwa usafi wake kamili wa toka mwanzo ulipotea." (Encyclopaedia of Religious Knowledge, Vol. 1).

2. "Kukubaliana wanazuoni wote wa Biblia ya kwamba Agano la Kale haliwezi kukubalika kama lilivyo kuwa ni taarifa sahihi ya historia linayoieleza, ni jambo linalowajibisha kubahatisha au kuleta mabahatisho ya mfululizo yatakayomwezesha mtu kusogelea kusoma habari zilizomo kitabuni humo za historia na za dini." (Palestine, Encyclopaedia Britanica, Vol. 20, uk. 615).

3. "Vitabu vitano vya kwanza vya Biblia, ni mkusanyiko wa maandiko kadha wa kadha ambayo kwanza yalikuwa hayategemeani, lakini mwishoni, pamoja na mapunguzo, mazidisho na mabadilisho kadha wa kadha, yakaunganishwa pamoja kufanya historia moja inayoendelea." (The Documents of the Hextateuch, page 14, by W. E. Addis, M.A., of Balilol College, Oxford).

4. "Agano Jipya mwanzo wake kabisa, halikuwa na mamlaka ya kutoa sheria, na mabadilisho na mazidisho kwa hakika yalifanywa yalipoonekana kuwa ndio kutengeneza vizuri." (Encyclopaedia Biblica Vol. 4, page 4980).

5. "Lakini, kwa hakika, kila Kitabu katika Agano Jipya, isipokuwa barua mashuhuri nne za Paulo Mt. leo hii kimekuwa kitu cha kufanyiwa ubishi, na mazidisho yanathibitishwa hata ndani ya Vitabu hivyo!" (Encyclopaedia Britannica, 13th Edn. Vol. 3, page 643).

6. "Hizo (hitilafu) zinatufanya tushindwe kabisa kuwa na hakika kama maneno tuliyo nayo katika kila hali ni hasa maneno ya Mtume au Mjumbe . . . . .

7. "Agano Jipya linaleta marejeo ya habari 228 kutoka Agano la Kale, na katika hizo ni habari 53 tu zinazopatana neno kwa neno." (Mordern Study of the Old Testment and Inspiration by T. H. Sprott, M.A., Padre wa Kanisa la Paulo Mt., Wellington, New Zealand).

Qur'an ilijua kazi hii ya mapadre na Mayahudi toka zamani, na ikawatanabahisha watu. Sasa hata Wakristo wenyewe hawaoni salama kunyamazia fujo hizo. Lakini je wataacha (Soma sura 2:43).

'Waswfah' - Kugeukia kando - kunaonyesha kitendo cha uvumilivu na kuyasamehe makosa ya watu wengine kwa huruma.

فَاَغۡرَيۡنَا بَيۡنَهُمُ الۡعَدَاوَةَ وَالۡبَغۡضَآءَ اِلٰى يَوۡمِ الۡقِيٰمَةِ ؕ وَسَوۡفَ يُنَبِّئُهُمُ اللّٰهُ بِمَا كَانُوۡا يَصۡنَعُوۡنَ ﴿۱۵﴾

lakini wakasahau sehemu ya yale waliyokumbushwa, kwa hiyo Tumeweka kati yao uadui na bughudha mpaka siku ya Kiyama. Na hivi karibuni Allah Atawaambia waliyokuwa wakiyafanya.

يٰۤاَهۡلَ الۡكِتٰبِ قَدۡ جَآءَكُمۡ رَسُوۡلُنَا يُبَيِّنُ لَكُمۡ كَثِيۡرًا مِّمَّا كُنۡتُمۡ تُخۡفُوۡنَ مِنَ الۡكِتٰبِ وَيَعۡفُوۡا عَنۡ كَثِيۡرٍ ؕ قَدۡ جَآءَكُمۡ مِّنَ اللّٰهِ نُوۡرٌ وَّكِتٰبٌ مُّبِيۡنٌ ۙ﴿۱۶﴾

16. Enyi watu wa Kitabu! hakika amekwisha wafikieni Mtume Wetu, huwadhihirishieni mengi mliyokuwa mkiyaficha katika Kitabu, na husamehe mengi. Bila shaka imekwisha wafikieni Nuru kutoka kwa Allah na Kitabu kinachobainisha.

يَّهۡدِىۡ بِهِ اللّٰهُ مَنِ اتَّبَعَ رِضۡوَانَهٗ سُبُلَ السَّلٰمِ وَيُخۡرِجُهُمۡ مِّنَ الظُّلُمٰتِ اِلَى النُّوۡرِ بِاِذۡنِهٖ وَيَهۡدِيۡهِمۡ اِلٰى صِرَاطٍ مُّسۡتَقِيۡمٍ ﴿۱۷﴾

17. Kwa (Kitabu) hicho Allah Humwongoza mwenye kufuata radhi Yake katika njia za salama, na Huwatoa katika giza kuwapeleka kwenye nuru kwa amri Yake, na kuwaongoza kwenye njia iliyonyooka.

لَقَدۡ كَفَرَ الَّذِيۡنَ قَالُوۡۤا اِنَّ اللّٰهَ هُوَ الۡمَسِيۡحُ ابۡنُ مَرۡيَمَ ؕ قُلۡ فَمَنۡ يَّمۡلِكُ مِنَ اللّٰهِ شَيۡـًٔا اِنۡ اَرَادَ اَنۡ يُّهۡلِكَ الۡمَسِيۡحَ ابۡنَ مَرۡيَمَ وَاُمَّهٗ وَمَنۡ فِى الۡاَرۡضِ جَمِيۡعًا ؕ وَلِلّٰهِ مُلۡكُ السَّمٰوٰتِ وَالۡاَرۡضِ وَمَا بَيۡنَهُمَا ؕ يَخۡلُقُ مَا يَشَآءُ ؕ وَاللّٰهُ عَلٰى كُلِّ شَىۡءٍ قَدِيۡرٌ ﴿۱۸﴾

18. Kwa yakini wamekwisha kufuru wale waliosema: Hakika Allah ni Masihi bin Mariam. Sema: Ni nani atakayemiliki cho chote mbele ya Allah kama yeye Angetaka kumwangamiza Masihi bin Mariam na mama yake, na vyote vilivyomo katika ardhi? Na ufalme wa mbingu na ardhi na vilivyomo kati yao ni wa Allah. Huumba Apendavyo. Na Allah Anao uwezo juu ya kila kitu.

وَقَالَتِ الْيَهُوْدُ وَالنَّصٰرٰى نَحْنُ اَبْنٰٓؤُا اللّٰهِ
وَاَحِبَّآؤُهٗ ؕ قُلْ فَلِمَ يُعَذِّبُكُمْ
بِذُنُوْبِكُمْ ؕ بَلْ اَنْتُمْ بَشَرٌ مِّمَّنْ خَلَقَ ؕ
يَغْفِرُ لِمَنْ يَّشَآءُ وَيُعَذِّبُ مَنْ يَّشَآءُ ؕ وَلِلّٰهِ
مُلْكُ السَّمٰوٰتِ وَالْاَرْضِ وَمَا بَيْنَهُمَا ۫
وَاِلَيْهِ الْمَصِيْرُ ﴿١٩﴾

19. Na Mayahudi na Wakristo wanasema: Sisi ni wana wa Allah na wapenzi Wake. Sema: Basi kwa nini tena Anawaadhibuni kwa ajili ya dhambi zenu? Bali ninyi ni watu tu katika wale Aliowaumba. Humghofiri Amtakaye na Humwadhibu Amtakaye. Na ufalme wa mbingu na ardhi na vilivyomo kati yao ni wa Allah; na marudio ni Kwake.

يٰٓاَهْلَ الْكِتٰبِ قَدْ جَآءَكُمْ رَسُوْلُنَا يُبَيِّنُ
لَكُمْ عَلٰى فَتْرَةٍ مِّنَ الرُّسُلِ اَنْ تَقُوْلُوْا مَا
جَآءَنَا مِنْۢ بَشِيْرٍ وَّلَا نَذِيْرٍ ۫ فَقَدْ
جَآءَكُمْ بَشِيْرٌ وَّنَذِيْرٌ ؕ وَاللّٰهُ عَلٰى كُلِّ
شَىْءٍ قَدِيْرٌ ﴿٢٠﴾ ع

20. Enyi watu wa Kitabu! bila shaka amewafikieni Mtume Wetu, huwabainishieni katika wakati usio na Mitume, msije mkasema, hakufika kwetu Mtoaji wa habari njema wala Mwonyaji; kwa hiyo amewafikieni Abashiriaye na Aonyaye, na Allah Anao uwezo juu ya kila kitu.

Aya 19. *Wana wa Allah.* Biblia imetumia neno hili mahali pengi na katika maana mbalimbali:-

(i) Pengine "wana wa Mungu" maana yake ni wapenzi Wake. Wana wa Israeli wameitwa wana wa Mungu katika maana hiyo (Kumbukumbu 14:1; Isiah 63:16; Jeremiah 3:4, 19; 1 Mambo ya Nyakati 29:10; Hosea 11:1). Waaminio pia wameitwa wana wa Mungu (Luka 20:36; Mattayo 5:18; Warumi 8:14-17; 1 Yohana 3:1, 2, 9; 4:7; 5:1,4; 2 Wakorintho 6:18).

(ii) Na pengine maana yake ni kiumbe tu. Watu wapotevu wameitwa wanawe (Kumbukumbu 32:19, 20); Wana wanaoasi (Isiah 30:1). Imeandikwa katika Mwanzo 6:2 "Wana wa Mungu waliwaona hao binti za wanadamu ya kuwa ni wazuri; wakajitwalia wake wo wote waliowachagua."

(iii) Manabii pia wamepewa jina hilo la "wana wa Mungu," kama Adamu (Luka 3:38), Sulemani (1 Mambo ya Nyakati 22:10; 28:6), na Yesu (Matei 3:17). Madai ya Mayahudi kuwa wana wa Mungu yameandikwa katika Injili pia. Tazama Yohana 8:41.

Anawaadhibuni. Mayahudi na Wakristo wamejibiwa kwamba ingawa wao ni wanawe na wapenzi Wake wanaadhibiwa duniani mara kwa mara kwa ajili ya madhambi yao, basi na huko Akhera pia watapata adhabu ya maovu yao wasipotubu na kuamini. Kujiita wanawe tu hakutafaa cho chote.

Aya 20. *Wakati usio na Mitume,* mradi wake: kabla ya Mtume s.a.w. hakukuwa Mtume aliyemtangulia karibu karibu.

FUNGU 4

وَاِذْ قَالَ مُوْسٰى لِقَوْمِهٖ يٰقَوْمِ اذْكُرُوْا نِعْمَةَ اللّٰهِ عَلَيْكُمْ اِذْ جَعَلَ فِيْكُمْ اَنْۢبِيَآءَ وَجَعَلَكُمْ مُّلُوْكًا ۖ وَّاٰتٰىكُمْ مَّا لَمْ يُؤْتِ اَحَدًا مِّنَ الْعٰلَمِيْنَ ﴿٢١﴾

21. Na (kumbukeni) Musa alipowaambia watu wake: Enyi watu wangu! Kumbukeni neema za Allah zilizo juu yenu, Alipowafanya Manabii kati yenu na Akawafanyeni wafalme, na Akawapeni ambayo Hakumpa yeyote katika walimwengu.

يٰقَوْمِ ادْخُلُوا الْاَرْضَ الْمُقَدَّسَةَ الَّتِيْ كَتَبَ اللّٰهُ لَكُمْ وَلَا تَرْتَدُّوْا عَلٰٓى اَدْبَارِكُمْ فَتَنْقَلِبُوْا خٰسِرِيْنَ ﴿٢٢﴾

22. Enyi watu wangu, ingieni katika ardhi iliyotakaswa ambayo Allah Amewaandikieni, wala msirudi nyuma, msije mkarudi wenye hasara.

قَالُوْا يٰمُوْسٰٓى اِنَّ فِيْهَا قَوْمًا جَبَّارِيْنَ ۖ وَاِنَّا لَنْ نَّدْخُلَهَا حَتّٰى يَخْرُجُوْا مِنْهَا ۚ فَاِنْ يَّخْرُجُوْا مِنْهَا فَاِنَّا دٰخِلُوْنَ ﴿٢٣﴾

23. Wakasema: Ewe Musa! Hakika huko kuna watu majabari. Nasi hatutaingia huko mpaka watoke humo; basi wao wakitoka humo, hapo bila shaka tutaingia.

قَالَ رَجُلٰنِ مِنَ الَّذِيْنَ يَخَافُوْنَ اَنْعَمَ اللّٰهُ عَلَيْهِمَا ادْخُلُوْا عَلَيْهِمُ الْبَابَ ۚ فَاِذَا دَخَلْتُمُوْهُ فَاِنَّكُمْ غٰلِبُوْنَ ۚ وَعَلَى اللّٰهِ فَتَوَكَّلُوْٓا اِنْ كُنْتُمْ مُّؤْمِنِيْنَ ﴿٢٤﴾

24. Watu wawili miongoni mwa wale walioogopa, ambao Allah Amewaneemesha, wakasema: Wavamieni kupitia mlangoni; maana mtakapowavamilia hapo, basi kwa yakini ninyi mtashinda. Na tegemeeni juu ya Allah ikiwa ninyi ni waaminio.

قَالُوْا يٰمُوْسٰٓى اِنَّا لَنْ نَّدْخُلَهَآ اَبَدًا مَّا دَامُوْا فِيْهَا فَاذْهَبْ اَنْتَ وَرَبُّكَ فَقَاتِلَآ اِنَّا هٰهُنَا قٰعِدُوْنَ ﴿٢٥﴾

25. Wakasema: Ewe Musa! Kwa yakini sisi hatutaingia humo kamwe maadamu wao wamo humo. Basi nenda wewe na Mola wako mkapigane, bila shaka sisi tunakaa hapa hapa.

Aya 21. Hapa neema mbili za Allah zimetajwa, (1) neema ya kiroho - Unabii; (2) neema za kidunia - Ufalme. Maneno 'ulimwenguni kote' yanahusikana na watu wa zama zile.

Aya 23. Linganisha maneno haya ya woga ya wafuasi wa Nabii Musa na kujitoa kwa ajabu kwa masahaba wa Mtume Muhammad *s.a.w.*, ambao kila wakati walikuwa tayari kujitupa katika mauti kwa kutimiza amri za Mtume *s.a.w.* Historia ya Kiislamu imejaa matukio ya namna hii ya masahaba kujisalimisha kabisa.

قَالَ رَبِّ اِنِّیۡ لَاۤ اَمۡلِكُ اِلَّا نَفۡسِیۡ وَاَخِیۡ فَافۡرُقۡ بَیۡنَنَا وَبَیۡنَ الۡقَوۡمِ الۡفٰسِقِیۡنَ ﴿۲۶﴾

26. (Musa) akasema: Mola wangu, hakika similiki ila nafsi yangu na ndugu yangu; basi Upambanue baina yetu na baina ya watu waasi.

قَالَ فَاِنَّهَا مُحَرَّمَةٌ عَلَیۡهِمۡ اَرۡبَعِیۡنَ سَنَةً ۚ یَتِیۡهُوۡنَ فِی الۡاَرۡضِ ؕ فَلَا تَاۡسَ عَلَی الۡقَوۡمِ الۡفٰسِقِیۡنَ ﴿۲۷﴾ ع

27. (Allah) Akasema: Basi kwa yakini wameiharamishiwa kwa (muda wa) miaka arobaini, watatangatanga ardhini. Basi usiwahuzunikie watu waasi.

FUNGU 5

وَاتۡلُ عَلَیۡهِمۡ نَبَاَ ابۡنَیۡۡ اٰدَمَ بِالۡحَقِّ ۘ اِذۡ قَرَّبَا قُرۡبَانًا فَتُقُبِّلَ مِنۡ اَحَدِهِمَا وَلَمۡ یُتَقَبَّلۡ مِنَ الۡاٰخَرِ ؕ قَالَ لَاَقۡتُلَنَّكَ ؕ قَالَ اِنَّمَا یَتَقَبَّلُ اللّٰهُ مِنَ الۡمُتَّقِیۡنَ ﴿۲۸﴾ ع

28. Na wasomee habari za watoto wawili wa Adamu kwa haki, walipotoa sadaka - basi ikakubaliwa ya mmoja wao na ya mwingine haikukubaliwa. Akasema: Bila shaka nitakuua. (Mwenziwe) akasema: Allah Huwapokelea wamchao tu.

لَئِنۡۢ بَسَطۡتَّ اِلَیَّ یَدَكَ لِتَقۡتُلَنِیۡ مَاۤ اَنَا بِبَاسِطٍ یَّدِیَ اِلَیۡكَ لِاَقۡتُلَكَ ۚ اِنِّیۡۤ اَخَافُ اللّٰهَ رَبَّ الۡعٰلَمِیۡنَ ﴿۲۹﴾

29. Kama utanyoosha mkono wako kwangu kuniua, mimi sitakunyooshea mkono wangu kukuua. Hakika mimi namwogopa Allah, Mola wa walimwengu.

اِنِّیۡۤ اُرِیۡدُ اَنۡ تَبُوۡٓاَ بِاِثۡمِیۡ وَاِثۡمِكَ فَتَكُوۡنَ مِنۡ اَصۡحٰبِ النَّارِ ۚ وَذٰلِكَ جَزٰٓؤُا الظّٰلِمِیۡنَ ﴿۳۰﴾ ۚ

30. Hakika mimi nataka ubebe dhambi yangu na dhambi yako, na kwa hiyo uwe miongoni mwa watu wa Motoni; na hayo ndio malipo ya wadhalimu.

فَطَوَّعَتۡ لَهٗ نَفۡسُهٗ قَتۡلَ اَخِیۡهِ فَقَتَلَهٗ فَاَصۡبَحَ مِنَ الۡخٰسِرِیۡنَ ﴿۳۱﴾

31. Basi nafsi yake ikamhimiza kumwua nduguye, ndipo akamwua; na akawa miongoni mwa wenye hasara.

Aya 27. Waisraeli walipoonyesha woga wa namna hii Allah Akakadiria wakae katika jangwa kwa miaka arobaini ili wapate nguvu na kuimarika tabia zao. Katika muda huo wazee walikwisha na wazao wa nyuma wakawa mashujaa wa kutosha kuishinda nchi waliyoahidiwa. Pia soma Biblia, (Hesabu mlango 14).

Aya 28. *Huwapokelea wamchao tu,* Maneno haya yanaonyesha jambo la maana sana ya kuwa sadaka isiyo na kiini cha uchaji wa moyo haina maana. Allah hajali maonyesho matupu ya nje; Yeye hupokea vile tu vinavyotolewa kwa nia safi.

فَبَعَثَ اللّٰهُ غُرَابًا يَّبْحَثُ فِي الْاَرْضِ لِيُرِيَهٗ كَيْفَ يُوَارِيْ سَوْءَةَ اَخِيْهِ ؕ قَالَ يٰوَيْلَتٰى اَعَجَزْتُ اَنْ اَكُوْنَ مِثْلَ هٰذَا الْغُرَابِ فَاُوَارِيَ سَوْءَةَ اَخِيْ ۚ فَاَصْبَحَ مِنَ النّٰدِمِيْنَ ۚ﴿۳۱﴾

32. Hapo Allah Akamtuma kunguru anayefukua katika ardhi, ili amuonyeshe jinsi ya kuisitiri maiti ya ndugu yake. Akasema: Ole wangu! Je, nimeshindwa kuwa sawa na kunguru huyu na kuistiri maiti ya ndugu yangu? Basi akawa miongoni mwa wajutao.

مِنْ اَجْلِ ذٰلِكَ ۛ كَتَبْنَا عَلٰى بَنِيْۤ اِسْرَآءِيْلَ اَنَّهٗ مَنْ قَتَلَ نَفْسًۢا بِغَيْرِ نَفْسٍ اَوْ فَسَادٍ فِي الْاَرْضِ فَكَاَنَّمَا قَتَلَ النَّاسَ جَمِيْعًا ؕ وَمَنْ اَحْيَاهَا فَكَاَنَّمَاۤ اَحْيَا النَّاسَ جَمِيْعًا ؕ وَلَقَدْ جَآءَتْهُمْ رُسُلُنَا بِالْبَيِّنٰتِ ۫ ثُمَّ اِنَّ كَثِيْرًا مِّنْهُمْ بَعْدَ ذٰلِكَ فِي الْاَرْضِ لَمُسْرِفُوْنَ ﴿۳۲﴾

33. Kwa sababu ya hayo Tukawaandikia wana wa Israeili ya kwamba atakayemuua mtu asiyeua mtu, au bila machafuko katika nchi, basi ni kama amewaua watu wote; na mwenye kumwacha (mtu) hai ni kama amewaacha hai watu wote. Na bila shaka Mitume wetu wameshawafikia na Ishara zilizo wazi, kisha wengi wao baada ya haya walikuwa waharibifu sana katika nchi.

اِنَّمَا جَزٰٓؤُا الَّذِيْنَ يُحَارِبُوْنَ اللّٰهَ وَرَسُوْلَهٗ وَيَسْعَوْنَ فِي الْاَرْضِ فَسَادًا اَنْ يُّقَتَّلُوْۤا اَوْ يُصَلَّبُوْۤا اَوْ تُقَطَّعَ اَيْدِيْهِمْ وَاَرْجُلُهُمْ مِّنْ خِلَافٍ اَوْ يُنْفَوْا مِنَ الْاَرْضِ ؕ ذٰلِكَ لَهُمْ خِزْيٌ فِي الدُّنْيَا وَلَهُمْ فِي الْاٰخِرَةِ عَذَابٌ عَظِيْمٌ ۙ﴿۳۳﴾

34. Hakika malipo ya wale wanaopigana na Allah na Mtume Wake na wafanyao fujo katika nchi, ni kuuawa au kusulubiwa au kukatwa mikono yao na miguu yao kwa kubadilishwa au kufukuzwa katika nchi; hii ndio fedheha kwao katika dunia, na katika Akhera watapata adhabu kubwa.

اِلَّا الَّذِيْنَ تَابُوْا مِنْ قَبْلِ اَنْ تَقْدِرُوْا عَلَيْهِمْ ۚ فَاعْلَمُوْۤا اَنَّ اللّٰهَ غَفُوْرٌ رَّحِيْمٌ ﴿۳۴﴾ ع ۸ ۹

35. Isipokuwa wale waliotubia kabla hamjawatia nguvuni; na jueni kwamba Allah ndiye Msamehevu, Mrehemevu.

Aya 34. Aya hii inaonyesha namna mbalimbali za adhabu zinazoweza kupewa watu wanaoleta vita kuwadhulumu bure Waislamu kwa kuwaua na kuwachinja na kueneza machafuko katika nchi. Aya hii inaonyesha ya kuwa dini ya Kiislamu haichelei kutoa adhabu zilizo kali inapokuwa zitawaletea watu au serikali faida.

FUNGU 6

يٰٓاَيُّهَا الَّذِيْنَ اٰمَنُوا اتَّقُوا اللّٰهَ وَابْتَغُوْٓا اِلَيْهِ الْوَسِيْلَةَ وَجَاهِدُوْا فِيْ سَبِيْلِهٖ لَعَلَّكُمْ تُفْلِحُوْنَ ﴿٣٦﴾

36. Enyi mlioamini! Mcheni Allah na tafuteni njia ya kuwa karibu naye, na jitahidini katika njia Yake ili mpate kufaulu.

اِنَّ الَّذِيْنَ كَفَرُوْا لَوْ اَنَّ لَهُمْ مَّا فِي الْاَرْضِ جَمِيْعًا وَّمِثْلَهٗ مَعَهٗ لِيَفْتَدُوْا بِهٖ مِنْ عَذَابِ يَوْمِ الْقِيٰمَةِ مَا تُقُبِّلَ مِنْهُمْ ۚ وَلَهُمْ عَذَابٌ اَلِيْمٌ ﴿٣٧﴾

37. Kwa yakini wale waliokufuru lau wangekuwa na yote yaliyomo duniani na mengine kama hayo, ili watoe fidia ya kuepukana na adhabu ya siku ya Kiyama, yasingelipokewa kwao, na watapata adhabu iumizayo.

يُرِيْدُوْنَ اَنْ يَّخْرُجُوْا مِنَ النَّارِ وَمَا هُمْ بِخٰرِجِيْنَ مِنْهَا ۡ وَلَهُمْ عَذَابٌ مُّقِيْمٌ ﴿٣٨﴾

38. Watapenda kutoka katika Moto lakini hawatatoka humo, na watakuwa na adhabu idumuyo.

وَالسَّارِقُ وَالسَّارِقَةُ فَاقْطَعُوْٓا اَيْدِيَهُمَا جَزَآءًۢ بِمَا كَسَبَا نَكَالًا مِّنَ اللّٰهِ ۭ وَاللّٰهُ عَزِيْزٌ حَكِيْمٌ ﴿٣٩﴾

39. Na mwizi mwanamume na mwizi mwanamke, basi ikateni mikono yao, malipo ya yale waliyoyachuma. Ndio adhabu itokayo kwa Allah, na Allah ni Mwenye nguvu, Mwenye hekima.

فَمَنْ تَابَ مِنْۢ بَعْدِ ظُلْمِهٖ وَاَصْلَحَ فَاِنَّ اللّٰهَ يَتُوْبُ عَلَيْهِ ۭ اِنَّ اللّٰهَ غَفُوْرٌ رَّحِيْمٌ ﴿٤٠﴾

40. Lakini mwenye kutubia baada ya dhuluma yake, na kutenda wema, basi bila shaka Allah Atapokea toba yake. Hakika Allah ni Msamehevu, Mrehemevu.

اَلَمْ تَعْلَمْ اَنَّ اللّٰهَ لَهٗ مُلْكُ السَّمٰوٰتِ وَالْاَرْضِ ۭ يُعَذِّبُ مَنْ يَّشَاۗءُ وَيَغْفِرُ لِمَنْ يَّشَاۗءُ ۭ وَاللّٰهُ عَلٰي كُلِّ شَيْءٍ قَدِيْرٌ ﴿٤١﴾

41. Je! Hujui ya kwamba Allah Anao ufalme wa mbingu na ardhi? Humwadhibu Amtakaye na Humsamehe Amtakaye, na Allah ni Mwenye uwezo juu ya kila kitu.

Aya 36. *Wasiila,* "Njia ya kuwa karibu." Si sawa kufasiri neno hili kuwa "mwamuzi aliyoko baina ya mtu na Allah." Mtume *s.a.w.* alisema, "Niombeeni *wasiila*," yaani niombeeni Mungu anipe namna ya pekee ya kuwa karibu naye. Na kila baada ya Adhana kuna dua ambayo pia ina maneno haya: "Ee Mola mpe Muhammad *wasiila,*" yaani amzidishiye sana ukaribu pamoja naye.

Aya 39. *Ikateni mikono yao.* Seyyidna Ali, mkwewe Mtume *s.a.w.* na ambaye alikuwa Khalifa wa nne, alifasiri neno *yad* (mkono) kuwa ni vidole vya mwizi vinavyotakiwa kukatwa

42. Ewe Mtume! Wasikuhuzunishe wale wafanyao haraka kukufuru, miongoni mwa wale waliosema, tumeamini, kwa vinywa vyao hali mioyo yao haiamini; na miongoni mwa Mayahudi pia wako wale ambao wana shauku iliyopita kiasi ya kusikiliza uwongo, wasikilizao kwa ajili ya watu wengine wasiokufikia; huyabadilisha maneno baada ya kuwa mahali pao; wanasema: Mkipewa hayo basi yashikeni, na msipopewa hayo basi jihadharini. Na mtu ambaye Allah Anataka kumjaribu, basi huwezi kumpatia mbele ya Allah cho chote. Hao ndio ambao Allah Hapendi kuitakasa mioyo yao. Watakuwa na fedheha duniani, na katika Akhera watakuwa na adhabu kubwa.

يٰٓاَيُّهَا الرَّسُوْلُ لَا يَحْزُنْكَ الَّذِيْنَ
يُسَارِعُوْنَ فِي الْكُفْرِ مِنَ الَّذِيْنَ قَالُوْٓا اٰمَنَّا
بِاَفْوَاهِهِمْ وَلَمْ تُؤْمِنْ قُلُوْبُهُمْ ۛ وَمِنَ
الَّذِيْنَ هَادُوْا ۛ سَمّٰعُوْنَ لِلْكَذِبِ
سَمّٰعُوْنَ لِقَوْمٍ اٰخَرِيْنَ ۙ لَمْ يَاْتُوْكَ ۭ
يُحَرِّفُوْنَ الْكَلِمَ مِنْۢ بَعْدِ مَوَاضِعِهٖ ۚ
يَقُوْلُوْنَ اِنْ اُوْتِيْتُمْ هٰذَا فَخُذُوْهُ وَاِنْ لَّمْ
تُؤْتَوْهُ فَاحْذَرُوْا ۭ وَمَنْ يُّرِدِ اللّٰهُ فِتْنَتَهٗ
فَلَنْ تَمْلِكَ لَهٗ مِنَ اللّٰهِ شَيْـــًٔا ۭ اُولٰۗىِٕكَ الَّذِيْنَ
لَمْ يُرِدِ اللّٰهُ اَنْ يُّطَهِّرَ قُلُوْبَهُمْ ۭ لَهُمْ فِي
الدُّنْيَا خِزْيٌ ۚ وَّلَهُمْ فِي الْاٰخِرَةِ عَذَابٌ
عَظِيْمٌ ۝۴۱

43. Wasikilizao sana uwongo, walao sana haramu. Basi wakikujia, wahukumu baina yao au jiepushe nao. Na ukijiepusha nao, basi wao hawatakudhuru cho chote. Na ukiwahukumu, basi utoe hukumu baina yao kwa uadilifu. Bila shaka Allah Huwapenda waadilifu.

سَمّٰعُوْنَ لِلْكَذِبِ اَكّٰلُوْنَ لِلسُّحْتِ ۭ
فَاِنْ جَاۗءُوْكَ فَاحْكُمْ بَيْنَهُمْ اَوْ
اَعْرِضْ عَنْهُمْ ۚ وَاِنْ تُعْرِضْ عَنْهُمْ
فَلَنْ يَّضُرُّوْكَ شَيْـــًٔا ۭ وَاِنْ حَكَمْتَ
فَاحْكُمْ بَيْنَهُمْ بِالْقِسْطِ ۭ اِنَّ اللّٰهَ يُحِبُّ
الْمُقْسِطِيْنَ ۝۴۲

44. Na watakuwekaje kuwa hakimu nao wanayo Taurati yenye hukumu za Allah ? Kisha baada ya hayo wanakengeuka; na hao si wenye kuamini.

وَكَيْفَ يُحَكِّمُوْنَكَ وَعِنْدَهُمُ التَّوْرٰىةُ
فِيْهَا حُكْمُ اللّٰهِ ثُمَّ يَتَوَلَّوْنَ مِنْۢ بَعْدِ ذٰلِكَ ۭ
وَمَآ اُولٰۗىِٕكَ بِالْمُؤْمِنِيْنَ ۝۴۳ ع

(Ma'aaani, II, 304); ambapo maulamaa wengi sana wanasema ya kuwa mkono ukatwe katika fundo. Adhabu hii imekusudiwa kuung'oa kabisa wizi. Kuona huruma za uwongo ni kuharibu watu wengi. Ni bora mwizi mmoja akatwe mkono kuliko kumpa adhabu ya huruma na kuwafanya watu wengi kuwa wezi. Katika utawala wa Kiislamu watu waliokatwa mikono walikuwa wachache sana, maana adhabu hii iliwaogopesha wengine, na wizi ukazuilika. Ikumbukwe ya kuwa neno *assaariq* (mwizi) maana yake ni mwizi aliyezoea.

FUNGU 7

إِنَّآ أَنزَلْنَا التَّوْرٰىةَ فِيهَا هُدًى وَّنُورٌ ۚ يَحْكُمُ بِهَا النَّبِيُّوْنَ الَّذِيْنَ اَسْلَمُوْا لِلَّذِيْنَ هَادُوْا وَالرَّبّٰنِيُّوْنَ وَالْاَحْبَارُ بِمَا اسْتُحْفِظُوْا مِنْ كِتٰبِ اللّٰهِ وَكَانُوْا عَلَيْهِ شُهَدَآءَ ۚ فَلَا تَخْشَوُا النَّاسَ وَاخْشَوْنِ وَلَا تَشْتَرُوْا بِاٰيٰتِيْ ثَمَنًا قَلِيْلًا ۭ وَمَنْ لَّمْ يَحْكُمْ بِمَآ اَنْزَلَ اللّٰهُ فَاُولٰۗىِٕكَ هُمُ الْكٰفِرُوْنَ ۝۴۴

45. Hakika Tuliteremsha Taurati yenye mwongozo na nuru; ambayo kwayo Manabii waliojisalimisha (kwa Allah) waliwahukumu Mayahudi: na watawa na maulamaa pia, kwa sababu walitakiwa kuhifadhi Kitabu cha Allah, nao walikuwa mashahidi juu yake. Basi msiwaogope watu bali Niogopeni (Mimi),wala msiziuze Aya Zangu kwa thamani ndogo: Na asiyehukumu kwa yale Aliyoyateremsha Allah, basi hao ndio makafiri.

وَكَتَبْنَا عَلَيْهِمْ فِيْهَآ اَنَّ النَّفْسَ بِالنَّفْسِ ۙ وَالْعَيْنَ بِالْعَيْنِ وَالْاَنْفَ بِالْاَنْفِ وَالْاُذُنَ بِالْاُذُنِ وَالسِّنَّ بِالسِّنِّ ۙ وَالْجُرُوْحَ قِصَاصٌ ۭ فَمَنْ تَصَدَّقَ بِهٖ فَهُوَ كَفَّارَةٌ لَّهٗ ۭ وَمَنْ لَّمْ يَحْكُمْ بِمَآ اَنْزَلَ اللّٰهُ فَاُولٰۗىِٕكَ هُمُ الظّٰلِمُوْنَ ۝۴۵

46. Na humo Tuliwaandikia ya kwamba mtu kwa mtu, na jicho kwa jicho, na pua kwa pua, na sikio kwa sikio, na jino kwa jino, na pia itakuwa kisasi katika majeraha. Lakini atakayesamehe, basi itakuwa kafara kwake; na asiyehukumu kwa yale Aliyoyateremsha Allah, basi hao ndio wadhalimu.

وَقَفَّيْنَا عَلٰٓي اٰثَارِهِمْ بِعِيْسَى ابْنِ مَرْيَمَ مُصَدِّقًا لِّمَا بَيْنَ يَدَيْهِ مِنَ التَّوْرٰىةِ ۠ وَاٰتَيْنٰهُ الْاِنْجِيْلَ فِيْهِ هُدًى وَّنُوْرٌ ۙ وَّمُصَدِّقًا لِّمَا بَيْنَ يَدَيْهِ مِنَ التَّوْرٰىةِ وَهُدًى وَّمَوْعِظَةً لِّلْمُتَّقِيْنَ ۝۴۶

47. Na Tukamfuatisha Isa bin Mariamu katika nyayo zao, kusadikisha yaliyokuwa kabla yake katika Taurati, na Tukampa Injili yenye mwongozo na nuru na isadikishayo yaliyokuwa kabla yake katika Taurati, na mwongozo na mawaidha kwa wamchao.

Aya 45. *Kwayo Manabii . . . waliwahukumu Mayahudi,* ni maneno yenye kuonyesha kuwa kuna Manabii ambao hawakuleta sheria mpya ila walikuja hukumu kwa kufuata kanuni ya Taurati. Manabii wote waliotokea katika Mayahudi baada ya Nabii Musa hawakuleta sheria mpya, bali walifuata sheria ya Taurati.

48. Na watu wa Injili wahukumu kwa yale Aliyoyateremsha Allah ndani yake; na asiyehukumu kwa yale Aliyoyateremsha Allah basi hao ndio waasi.

وَلْيَحْكُمْ اَهْلُ الْاِنْجِيْلِ بِمَآ اَنْزَلَ اللّٰهُ فِيْهِ ؕ وَمَنْ لَّمْ يَحْكُمْ بِمَآ اَنْزَلَ اللّٰهُ فَاُولٰٓئِكَ هُمُ الْفٰسِقُوْنَ ﴿٤٧﴾

49. Na Tumekuteremshia Kitabu kwa haki, kinachosadikisha yaliyokuwa kabla yake katika Kitabu, na kukihifadhi, basi uwahukumu baina yao kwa yale Aliyoyateremsha Allah, wala usifuate matamanio yao kwa kuacha haki iliyokufikia; kila mmoja wenu Tumemjaalia desturi na njia maalumu; na kama Allah Angalipenda Angewafanyeni kundi moja, lakini Anataka kuwajaribuni kwa hayo aliyowapeni. Basi shindaneni katika mambo ya heri. Ninyi nyote marudio yenu ni kwa Allah; naye Atawaambieni yale mliyokuwa mkihitilafiana.

وَاَنْزَلْنَآ اِلَيْكَ الْكِتٰبَ بِالْحَقِّ مُصَدِّقًا لِّمَا بَيْنَ يَدَيْهِ مِنَ الْكِتٰبِ وَمُهَيْمِنًا عَلَيْهِ فَاحْكُمْ بَيْنَهُمْ بِمَآ اَنْزَلَ اللّٰهُ وَلَا تَتَّبِعْ اَهْوَآءَهُمْ عَمَّا جَآءَكَ مِنَ الْحَقِّ ؕ لِكُلٍّ جَعَلْنَا مِنْكُمْ شِرْعَةً وَّمِنْهَاجًا ؕ وَلَوْ شَآءَ اللّٰهُ لَجَعَلَكُمْ اُمَّةً وَّاحِدَةً وَّلٰكِنْ لِّيَبْلُوَكُمْ فِيْ مَآ اٰتٰىكُمْ فَاسْتَبِقُوا الْخَيْرٰتِ ؕ اِلَى اللّٰهِ مَرْجِعُكُمْ جَمِيْعًا فَيُنَبِّئُكُمْ بِمَا كُنْتُمْ فِيْهِ تَخْتَلِفُوْنَ ﴿٤٨﴾

50. Na uwahukumu baina yao kwa yale aliyoyateremsha Allah, wala usi fuate matamanio yao, nawe jihadhari nao wasije kukugeuza katika baadhi ya yale Aliyokuteremshia Allah; na kama wakigeuka,

وَاَنِ احْكُمْ بَيْنَهُمْ بِمَآ اَنْزَلَ اللّٰهُ وَلَا تَتَّبِعْ اَهْوَآءَهُمْ وَاحْذَرْهُمْ اَنْ يَّفْتِنُوْكَ عَنْۢ بَعْضِ مَآ اَنْزَلَ اللّٰهُ

Aya 48. Maneno ya Aya hii na yaliyomo katika Aya 45 na 47 ya sura hii hayaamrishi watu kufuata Sheria ya Mussa au ya Isa, bali yanahusu bishara zilizomo katika Taurati na Injili zinazoeleza kufika kwa Mtume Muhammad *s.a.w.* Hivyo Mayahudi na Wakristo wanaonywa ya kuwa wakizipinza bishara hizo na kumkataa Mtume *s.a.w.* wataonekana ni waasi mbele ya Allah.

Aya 49. *Kukihifadhi.* Qur'an inahifadhi Biblia kwa namna *tatu* :-

1. Imekusanya maneno yote mazuri na yenye kudumu siku zote yaliyopatikana katika vyuo vya zamani.

2. Inaeleza mageuzi yaliyofanywa na wafuasi wa Sheria hiyo katika Vyuo vyao.

3. Inatoa mafundisho mapya yanayohitajika kwa kuwaongoza watu mpaka siku ya Mwisho na kuinua hali zao kwa namna zote.

اِلَيْكَ ؕ فَاِنْ تَوَلَّوْا فَاعْلَمْ اَنَّمَا يُرِيْدُ اللّٰهُ اَنْ يُّصِيْبَهُمْ بِبَعْضِ ذُنُوْبِهِمْ ؕ وَاِنَّ كَثِيْرًا مِّنَ النَّاسِ لَفٰسِقُوْنَ ﴿۴۹﴾

basi jua ya kwamba hakika Allah Anataka kuwafikishia (adhabu) kwa baadhi ya dhambi zao; na bila shaka wengi katika watu ni waasi.

اَفَحُكْمَ الْجَاهِلِيَّةِ يَبْغُوْنَ ؕ وَمَنْ اَحْسَنُ مِنَ اللّٰهِ حُكْمًا لِّقَوْمٍ يُّوْقِنُوْنَ ﴿۵۰﴾ ع ۱۱

51. Je! wao wanataka hukumu ya (siku za) ujinga? Na nani aliye mwema zaidi kuliko Allah katika hukumu kwa watu wenye yakini?

FUNGU 8

يٰۤاَيُّهَا الَّذِيْنَ اٰمَنُوْا لَا تَتَّخِذُوا الْيَهُوْدَ وَالنَّصٰرٰۤى اَوْلِيَآءَ ۘ بَعْضُهُمْ اَوْلِيَآءُ بَعْضٍ ؕ وَمَنْ يَّتَوَلَّهُمْ مِّنْكُمْ فَاِنَّهٗ مِنْهُمْ ؕ اِنَّ اللّٰهَ لَا يَهْدِى الْقَوْمَ الظّٰلِمِيْنَ ﴿۵۱﴾

52. Enyi mlioamini msiwafanye Mayahudi na Wakristo kuwa marafiki; wao kwa wao ni marafiki; na miongoni mwenu atakayefanya urafiki nao, basi huyu yu pamoja nao; hakika Allah Hawaongozi watu wadhalimu.

فَتَرَى الَّذِيْنَ فِىْ قُلُوْبِهِمْ مَّرَضٌ يُّسَارِعُوْنَ فِيْهِمْ يَقُوْلُوْنَ نَخْشٰۤى اَنْ تُصِيْبَنَا دَآئِرَةٌ ؕ فَعَسَى اللّٰهُ اَنْ يَّاْتِىَ بِالْفَتْحِ اَوْ اَمْرٍ مِّنْ عِنْدِهٖ فَيُصْبِحُوْا عَلٰى مَاۤ اَسَرُّوْا فِىْۤ اَنْفُسِهِمْ نٰدِمِيْنَ ﴿۵۲﴾

53. Lakini utawaona wale wenye ugonjwa mioyoni mwao wanakimbilia kwao wakisema: Tunaogopa tusije pata msiba. Lakini inamkinika ya kwamba Allah Alete ushindi au jambo jingine litokalo Kwake, na wawe wenye majuto juu ya yale waliyoyaficha katika nafsi zao.

وَيَقُوْلُ الَّذِيْنَ اٰمَنُوْۤا اَهٰۤؤُلَآءِ الَّذِيْنَ اَقْسَمُوْا بِاللّٰهِ جَهْدَ اَيْمَانِهِمْ ۙ اِنَّهُمْ لَمَعَكُمْ ؕ حَبِطَتْ اَعْمَالُهُمْ فَاَصْبَحُوْا خٰسِرِيْنَ ﴿۵۳﴾ ع

54. Na walioamini husema: Je, hao ndio waliomuapa Allah kwa viapo vyao vigumu, ya kwamba hakika wao wa pamoja nanyi? Vitendo vyao vimeharibika na wakawa wenye hasara.

يٰۤاَيُّهَا الَّذِيْنَ اٰمَنُوْا مَنْ يَّرْتَدَّ مِنْكُمْ عَنْ دِيْنِهٖ فَسَوْفَ يَاْتِى اللّٰهُ بِقَوْمٍ يُّحِبُّهُمْ وَيُحِبُّوْنَهٗۤ ۙ اَذِلَّةٍ عَلَى الْمُؤْمِنِيْنَ اَعِزَّةٍ عَلَى الْكٰفِرِيْنَ ۫ يُجَاهِدُوْنَ فِىْ سَبِيْلِ اللّٰهِ

55. Enyi mlioamini! atakayeicha miongoni mwenu dini yake, basi kwa yakini Allah Ataleta watu ambao Atawapenda nao watampenda, wapole kwa waaminio, wakali kwa makafiri. Watajitahidi katika njia ya Allah, wala

وَلَا يَخَافُوْنَ لَوْمَةَ لَآئِمٍ ؕ ذٰلِكَ فَضْلُ اللّٰهِ يُؤْتِيْهِ مَنْ يَّشَآءُ ؕ وَاللّٰهُ وَاسِعٌ عَلِيْمٌ ﴿٥٥﴾

hawataogopa lawama ya anayelaumu. Hiyo ni fadhili ya Allah, Humpa Amtakaye; na Allah ni Mwenye wasaa, Mwenye kujua.

اِنَّمَا وَلِيُّكُمُ اللّٰهُ وَرَسُوْلُهٗ وَالَّذِيْنَ اٰمَنُوا الَّذِيْنَ يُقِيْمُوْنَ الصَّلٰوةَ وَيُؤْتُوْنَ الزَّكٰوةَ وَهُمْ رٰكِعُوْنَ ﴿٥٦﴾

56. Kwa hakika rafiki yenu ni Allah tu, na Mtume Wake na waaminio ambao husimamisha Sala na hutoa Zaka nao ni wanyenyekeao (mbele ya Allah).

وَمَنْ يَّتَوَلَّ اللّٰهَ وَرَسُوْلَهٗ وَالَّذِيْنَ اٰمَنُوْا فَاِنَّ حِزْبَ اللّٰهِ هُمُ الْغٰلِبُوْنَ ﴿٥٧﴾ ع

57. Na atakayefanya urafiki na Allah na Mtume Wake na walioamini, basi kwa yakini kundi la Allah ndio wenye kushinda.

FUNGU 9

يٰۤاَيُّهَا الَّذِيْنَ اٰمَنُوْا لَا تَتَّخِذُوا الَّذِيْنَ اتَّخَذُوْا دِيْنَكُمْ هُزُوًا وَّلَعِبًا مِّنَ الَّذِيْنَ اُوْتُوا الْكِتٰبَ مِنْ قَبْلِكُمْ وَالْكُفَّارَ اَوْلِيَآءَ ۚ وَاتَّقُوا اللّٰهَ اِنْ كُنْتُمْ مُّؤْمِنِيْنَ ﴿٥٨﴾

58. Enyi mlioamini! Msiwafanye marafiki wale walioifanyia mzaha na mchezo dini yenu miongoni mwa wale waliopewa Kitabu kabla yenu na makafiri. Na mcheni Allah kama ninyi ni waaminio.

وَاِذَا نَادَيْتُمْ اِلَى الصَّلٰوةِ اتَّخَذُوْهَا هُزُوًا وَّلَعِبًا ؕ ذٰلِكَ بِاَنَّهُمْ قَوْمٌ لَّا يَعْقِلُوْنَ ﴿٥٩﴾

59. Na mnapoita kwenye Sala wanaifanyia mzaha na mchezo. Hayo ni kwa sababu wao ni watu wasio na akili.

قُلْ يٰۤاَهْلَ الْكِتٰبِ هَلْ تَنْقِمُوْنَ مِنَّاۤ اِلَّاۤ اَنْ اٰمَنَّا بِاللّٰهِ وَمَاۤ اُنْزِلَ اِلَيْنَا وَمَاۤ اُنْزِلَ مِنْ قَبْلُ ۙ وَاَنَّ اَكْثَرَكُمْ فٰسِقُوْنَ ﴿٦٠﴾

60. Sema: Enyi watu wa Kitabu! Je, mnatuona na makosa kwa sababu tu tumemwamini Allah na yale tuliyoteremshiwa zamani, na ya kwamba wengi wenu ni waasi?

قُلْ هَلْ اُنَبِّئُكُمْ بِشَرٍّ مِّنْ ذٰلِكَ مَثُوْبَةً عِنْدَ اللّٰهِ ؕ مَنْ لَّعَنَهُ اللّٰهُ وَغَضِبَ عَلَيْهِ

61. Sema: Je, niwaambieni yule ambaye ni mwenye malipo mabaya zaidi kuliko hayo mbele ya Allah? Ni Ambaye Allah

---

Aya 57. Watu hutafuta kufanya urafiki na watu wakubwa ili wafanikiwe katika maisha. Lakini Aya hii ni kama anauliza swali, ni nani mkubwa kuliko Allah na Mjumbe wake na waaminio wa kweli, na watakosaje kufanikiwa hao watakaofanya urafiki nao?

Aya 61. *Kuwa nyani na nguruwe.* Maneno haya yametumiwa kwa namna ya mfano. Siyo kwa kutukana, maana Qur'an haitumii matusi. Yametumiwa kuonyesha ilivyokuwa hali ya

وَجَعَلَ مِنْهُمُ الْقِرَدَةَ وَالْخَنَازِيْرَ وَعَبَدَ
الطَّاغُوْتَ ؕ اُولٰٓئِكَ شَرٌّ مَّكَانًا وَّاَضَلُّ
عَنْ سَوَآءِ السَّبِيْلِ ﴿٦٠﴾

Amemlaani na kumkasirikia, na Amefanya wengine wao kuwa nyani na nguruwe, na akamwabudu shetani. Hao ndio wenye mahali pabaya, na wapotevu sana katika njia iliyo sawa.

وَاِذَا جَآءُوْكُمْ قَالُوْٓا اٰمَنَّا وَقَدْ دَّخَلُوْا
بِالْكُفْرِ وَهُمْ قَدْ خَرَجُوْا بِهٖ ؕ وَاللّٰهُ اَعْلَمُ
بِمَا كَانُوْا يَكْتُمُوْنَ ﴿٦١﴾

62. Na wanapowafikieni husema: Tumeamini; hali wao wameingia pamoja na kufuru na wametoka nayo! Na Allah Huyafahamu sana waliyokuwa wakiyaficha.

وَتَرٰى كَثِيْرًا مِّنْهُمْ يُسَارِعُوْنَ فِى الْاِثْمِ
وَالْعُدْوَانِ وَاَكْلِهِمُ السُّحْتَ ؕ لَبِئْسَ مَا
كَانُوْا يَعْمَلُوْنَ ﴿٦٢﴾

63. Na utawaona wengi wao wanakimbilia kwenye dhambi na uasi na ulaji wao wa haramu. Bila shaka waliyokuwa wakiyafanya ni mabaya.

لَوْلَا يَنْهٰهُمُ الرَّبّٰنِيُّوْنَ وَالْاَحْبَارُ عَنْ
قَوْلِهِمُ الْاِثْمَ وَاَكْلِهِمُ السُّحْتَ ؕ لَبِئْسَ
مَا كَانُوْا يَصْنَعُوْنَ ﴿٦٣﴾

64. Mbona watu watawa na wanazuoni hawawakatazi maneno yao ya dhambi na ulaji wao wa haramu? Bila shaka waliyokuwa wakiyatenda ni mabaya.

وَقَالَتِ الْيَهُوْدُ يَدُ اللّٰهِ مَغْلُوْلَةٌ ؕ غُلَّتْ
اَيْدِيْهِمْ وَلُعِنُوْا بِمَا قَالُوْا ۘ بَلْ يَدٰهُ
مَبْسُوْطَتٰنِ ۙ يُنْفِقُ كَيْفَ يَشَآءُ ؕ
وَلَيَزِيْدَنَّ كَثِيْرًا مِّنْهُمْ مَّآ اُنْزِلَ اِلَيْكَ
مِنْ رَّبِّكَ طُغْيَانًا وَّكُفْرًا ؕ وَاَلْقَيْنَا
بَيْنَهُمُ الْعَدَاوَةَ وَالْبَغْضَآءَ اِلٰى يَوْمِ
الْقِيٰمَةِ ؕ كُلَّمَآ اَوْقَدُوْا نَارًا لِّلْحَرْبِ
اَطْفَاَهَا اللّٰهُ ۙ وَيَسْعَوْنَ فِى الْاَرْضِ
فَسَادًا ؕ وَاللّٰهُ لَا يُحِبُّ الْمُفْسِدِيْنَ ﴿٦٤﴾

65. Na Mayahudi wanasema: Mkono wa Allah umefumba. (Siyo, bali) mikono yao ndio iliyofumba, na wamelaaniwa kwa sababu ya yale waliyoyasema. Lakini mikono yake ndio iliyofumbuka, Hutoa Apendavyo. Kwa yakini yaliyoteremshwa Kwako kutoka kwa Mola Wako yatawazidisha wengi wao katika uasi na kufuru. Na Tumetia kati yao uadui na bughudha mpaka siku ya Kiyama; kila mara wanapowasha moto wa vita Allah Anauzimisha, na wanajitahidi kuleta uharibifu katika ardhi; na Allah Hawapendi waharibifu.

---

tabia ya Mayahudi. Tabia ya nyani inaelezwa na methali maarufu ya Kiarabu isemayo, "Huyo ni mzinifu zaidi kuliko nyani" na Yesu aliwaita Mayahudi, "Kizazi kibaya cha zinaa" (Matt. 12:39). Kadhalika nyani anajulikana sana kwa kuiga na kufanya dhihaka. Kadhalika nyani anajulikana kwa tabia za uchafu na tabia zisizo na haya na pia kwa upumbavu wake. Pia tazama sura 2:174.

66. Na kama watu wa Kitabu wangaliamini na kumcha Allah, bila shaka Tungaliwafutia madhambi yao na kuwaingiza katika Bustani zenye neema.

وَلَوْ اَنَّ اَهْلَ الْكِتٰبِ اٰمَنُوْا وَ اتَّقَوْا
لَكَفَّرْنَا عَنْهُمْ سَيِّاٰتِهِمْ وَ لَاَدْخَلْنٰهُمْ
جَنّٰتِ النَّعِيْمِ ﴿٦٥﴾

67. Na kama wangalisimamisha Taurati na Injili na yale yaliyoteremshwa kwao kutoka kwa Mola wao, kwa yakini wangalikula vya juu yao na vya chini ya miguu yao; wako watu miongoni mwao washikao njia ya katikati, lakini wengi wao wanayoyafanya ni mabaya.

وَلَوْ اَنَّهُمْ اَقَامُوا التَّوْرٰىةَ وَالْاِنْجِيْلَ وَمَآ
اُنْزِلَ اِلَيْهِمْ مِّنْ رَّبِّهِمْ لَاَكَلُوْا مِنْ
فَوْقِهِمْ وَمِنْ تَحْتِ اَرْجُلِهِمْ ؕ مِنْهُمْ
اُمَّةٌ مُّقْتَصِدَةٌ ؕ وَكَثِيْرٌ مِّنْهُمْ سَآءَ
مَا يَعْمَلُوْنَ ﴿٦٦﴾ ع

Aya 67. *Wangalisimamisha Taurati,* Mayahudi na Wakristo wameambiwa kusimamisha Taurati, Injili na Qur'an. Hayo yanawezekana hivi: (1) Mayahudi na Wakristo wafuate yale maneno ambayo yalitabiri kufika kwake Mtume s.a.w. Hizo bishara zinapatikana katika Taurati na Injili nazo zimeelezwa chini ya sura 7:158. Inaonekana kana kwamba Biblia yenyewe inamwongoza Myahudi au Mkristo moja kwa moja mpaka kwa Mtume *s.a.w.* Wakristo wanasema, Taurati inaaguwa kuzaliwa kwake Yesu na Waislamu husema Biblia nzima inaashiria kufika kwa Mtume Muhammad *s.a.w.* Ndio haki ijapo Wakristo waichukie jinsi wachukiavyo Mayahudi wanapoonyeshwa bishara za Yesu katika Taurati.

(2) Kuna mambo mengi yanayofanana katika sheria za Allah. Biblia na Qur'an zinapatana katika amri nyingi ambazo Mayahudi na Wakristo wanazivunja. Basi Aya hii inawaita kufuata amri hizo. Ndivyo wataweza kushika maagizo ya Vyuo vyao na ya Qur'an pia. Ni hekima ya Qur'an kuwaita watu wa Kitabu kwenye mwongozo kwa njia isiyo ngumu kwao. Baadhi ya mambo yale ni haya:

(i)Kumtii Mungu na kuasi kila amri iliyo kinyume na Sheria Yake.Mayahudi waliwatii wakuu wao sana na kuwapa heshima kama Mungu. Wakristo wanafuata amri za Maaskofu na Mapapa zaidi kuliko amri ya Allah. Hasa Wakatoliki wanatanguliza amri za Kanisa na kutojali Biblia.

(ii) Biblia imekataza uzinifu, tamaa, uuaji na mengineyo, na Mayahudi na Wakristo hawakutaka kujiepusha nayo. Jeremiah kinasema, "Nawezaje kukusamehe? Watoto wako wameniacha mimi, nao wameapa kwa hao ambao si miungu kitu: nilipokuwa nimewashibisha chakula, walizini, na kukutana pamoja makundi makundi hapo penye nyumba za makahaba" (5:7). Kinasema tena: "Lau kwamba huko bara nilikuwa na pahali pa kulala kwa hao watu wasafirio; ili nipate waacha hao watu wangu, nami niondoke kwao! Kwani wao ni wazinifu wote, ni mkutano wa watu waume wadanganyao. Nao wapeta ndimi zao kama ni uta wao ili kunena uwongo" (9:2-3).

Paulo aliandika, "Yakini habari imeenea ya kuwa kwenu kuna zinaa, na zinaa ya namna isiyokuweko hata katika Mataifa, kwamba mtu awe na mke wa babaye. Nanyi mwajivuna, wala hamkusikitika, ili kwamba aondolewe miongoni mwenu huyo aliyetenda jambo hilo." (1 Wakorintho 5:1-2). Tena Paulo alisema, "Lakini ikiwa kweli ya Mungu imezidi kudhihirisha utukufu wake kwa sababu ya uwongo wangu, mbona mimi ningali nahukumiwa kuwa ni mwenye dhambi?" (Warumi 3:7).

Canon H. J. E. Butcher akieleza hali ya watu wa Kitabu ilivyokuwa katika siku za Mtume

FUNGU 10

68. Ewe Mtume! Fikisha uliyoteremshiwa kutoka kwa Mola wako; na kama hutafanya, basi hukufikisha ujumbe Wake; na Allah Atakulinda na watu; hakika Allah hawaongozi watu wanaokufuru.

يٰٓاَيُّهَا الرَّسُوْلُ بَلِّغْ مَآ اُنْزِلَ اِلَيْكَ مِنْ رَّبِّكَ ؕ وَاِنْ لَّمْ تَفْعَلْ فَمَا بَلَّغْتَ رِسَالَتَهٗ ؕ وَاللّٰهُ يَعْصِمُكَ مِنَ النَّاسِ ؕ اِنَّ اللّٰهَ لَا يَهْدِى الْقَوْمَ الْكٰفِرِيْنَ ﴿٦٨﴾

69. Sema: Enyi watu wa Kitabu, hamko juu ya cho chote mpaka msimamishe Taurati na Injili, na yaliyoteremshwa kwenu kutoka kwa Mola wenu. Na bila shaka yaliyoteremshwa kwako kutoka kwa Mola wako yatawazidisha wengi wao katika uasi na kufuru. Basi usiwasikitikie watu wanaokufuru.

قُلْ يٰٓاَهْلَ الْكِتٰبِ لَسْتُمْ عَلٰى شَىْءٍ حَتّٰى تُقِيْمُوا التَّوْرٰىةَ وَالْاِنْجِيْلَ وَمَآ اُنْزِلَ اِلَيْكُمْ مِّنْ رَّبِّكُمْ ؕ وَلَيَزِيْدَنَّ كَثِيْرًا مِّنْهُمْ مَّآ اُنْزِلَ اِلَيْكَ مِنْ رَّبِّكَ طُغْيَانًا وَّكُفْرًا ۚ فَلَا تَاْسَ عَلَى الْقَوْمِ الْكٰفِرِيْنَ ﴿٦٩﴾

---

s.a.w. anasema, "Lakini zamani zile Kanisa la Kikristo lilikuwa gizani, na dini ya Kiyahudi ilikuwa haina uhai ndani yake." (Historia ya Kanisa uk. 85).

(iii) Mapadre waligeuza amri ya talaka iliyoruhusiwa katika Taurati na Injili (Kumbukumbu 24:1 na Matei 19:9), na wakatangaza kwamba kumpa talaka mwanamke ni dhambi. Amri ya kutahiri iliyotolewa na Mungu katika Taurati (Walawi 12:3) ilipuuzwa (1 Wakorintho 7:19). Nguruwe na nyamafu iliyoharimishwa na Mwenyezi Mugnu (Kumbukumbu 14:4) ilitakaswa na Paulo aliyesema, "Mtu mmoja anayo imani, anakula vyote; lakini yeye aliye dhaifu anakula mboga" (Warumi 14:2). Kuoa wake zaidi kulikoruhusiwa na Taurati (Kumbukumbu 25:5-9) kukaachwa.

Kweli Wakristo na Mayahudi walitupilia mbali Taurati na Injili ndio maana waliambiwa yale yaliyowashtusha. Kama washike Sheria yao inaelekea zaidi watasogea karibu na Uislamu na kuukubali.

Wangalikula vya juu yao. Wangepata baraka za kimbingu kama wahyi na kuzungumza na Allah na pia ustawi wa kidunia. Wangepata mvua nyingi za majira na pia ardhi ingewapa mazao yake kwa wingi: kwa neno zima Allah angewapa maendeleo ya kiroho na ya kidunia.

Aya 68. *Atakulinda na watu.* Ibni Jarir, Ibni Kathir, Durri Manthur na Al-Bahrul-Muhit vinaonyesha jumla kubwa ya waelezaji wanaosimulia ya kwamba Aya hii iliteremshwa Makka. Kuna wengine wanaosema Aya hii iliteremshwa Madina. Mtungaji wa Ruuhul-Ma'aani anasema, kwanza Aya hii iliteremshwa Makka na ikateremshwa tena Madina, na hii inaonekana kuwa sawa. Kwa hakika Aya hii inaonekana iliteremshwa mara nne au mara tano.

Ingawa maadui wa Islam walifanya kila juhudi kumwua Mtume *s.a.w.* lakini hawakufanikiwa. Toka mwanzo Allah alitoa ahadi kuwa atamlinda na akaikariri ahadi ile. Nasi tunaona maadui zake waliokuwa na nguvu kubwa walianguka mmoja mmoja, naye akabaki anasimama kama mwamba. Hivi ndivyo Allah anavyotimiza ahadi Zake, na anayelindwa na Allah tu ndiye hakika yuko salama.

70. Hakika wale walioamini na Mayahudi na Masabii na Wakristo - atakayemwamini Allah na siku ya Mwisho na kufanya vitendo vizuri - basi hao hawatakuwa na hofu wala hawata-huzunika.

إِنَّ الَّذِينَ آمَنُوا وَالَّذِينَ هَادُوا وَالصَّابِئُونَ
وَالنَّصَارَىٰ مَنْ آمَنَ بِاللَّهِ وَالْيَوْمِ الْآخِرِ
وَعَمِلَ صَالِحًا فَلَا خَوْفٌ عَلَيْهِمْ وَلَا هُمْ
يَحْزَنُونَ ﴿٧٠﴾

71. Kwa yakini Tulishika ahadi ya wana wa Israeli na Tukawapelekea Mitume. Kila mara alipowafikia Mtume kwa yale zisiyoyapenda nafsi zao, kundi moja wakalikadhibisha na kundi jingine wakaliua.

لَقَدْ أَخَذْنَا مِيثَاقَ بَنِي إِسْرَائِيلَ وَأَرْسَلْنَا
إِلَيْهِمْ رُسُلًا ۖ كُلَّمَا جَاءَهُمْ رَسُولٌ بِمَا
لَا تَهْوَىٰ أَنْفُسُهُمْ ۙ فَرِيقًا كَذَّبُوا
وَفَرِيقًا يَقْتُلُونَ ﴿٧١﴾

72. Na walidhani ya kwamba hai-tatokea adhabu, basi wakawa vipofu na viziwi; kisha Allah Akawapokelea toba zao, tena wengi wao wakawa vipofu na viziwi; na Allah Anayaona wanayoyatenda.

وَحَسِبُوا أَلَّا تَكُونَ فِتْنَةٌ فَعَمُوا
وَصَمُّوا ثُمَّ تَابَ اللَّهُ عَلَيْهِمْ ثُمَّ عَمُوا
وَصَمُّوا كَثِيرٌ مِنْهُمْ ۚ وَاللَّهُ بَصِيرٌ بِمَا
يَعْمَلُونَ ﴿٧٢﴾

73. Bila shaka wamekufuru wale waliosema, Hakika Allah ni Masihi bin Mariamu, na Masihi alisema: Enyi wana wa Israeli, Mwabuduni Allah , Mola wangu na Mola wenu, Kwa yakini anayemshirikisha Allah, hakika Allah Amemharamishia Pepo, na mahali pake ni Motoni; na wadhalimu hawatakuwa na wasaidizi.

لَقَدْ كَفَرَ الَّذِينَ قَالُوا إِنَّ اللَّهَ هُوَ الْمَسِيحُ
ابْنُ مَرْيَمَ ۖ وَقَالَ الْمَسِيحُ يَا بَنِي
إِسْرَائِيلَ اعْبُدُوا اللَّهَ رَبِّي وَرَبَّكُمْ ۖ إِنَّهُ
مَنْ يُشْرِكْ بِاللَّهِ فَقَدْ حَرَّمَ اللَّهُ عَلَيْهِ الْجَنَّةَ
وَمَأْوَاهُ النَّارُ ۖ وَمَا لِلظَّالِمِينَ مِنْ
أَنْصَارٍ ﴿٧٣﴾

74. Kwa hakika wamekufuru wale waliosema: Hakika Allah ni wa tatu wa watatu, hali hakuna mungu ila Mungu Mmoja. Na kama hawataacha

لَقَدْ كَفَرَ الَّذِينَ قَالُوا إِنَّ اللَّهَ ثَالِثُ
ثَلَاثَةٍ ۘ وَمَا مِنْ إِلَٰهٍ إِلَّا إِلَٰهٌ وَاحِدٌ ۚ

Aya 73. Habari hii ya kusema Yesu aliwafunza Waisraeli wamwabudu Mungu peke Yake inaonekana hata katika hizi Injili zilizo katika hali ya kugeuzwa-geuzwa (Kwa mfano Matt. 4:10; Luka 4:8). Pia tazama sura 5:18.

Aya 74. Aya hii inaeleza fundisho la Utatu la dini ya Kikristo - fundisho hili lisilofahamika la nafsi tatu za Uungu - Baba, Mwana na Roho Mtakatifu - walio pamoja milele na wasio sawa

hayo wayasemayo, kwa yakini itawagusa wale waliokufuru miongoni mwao adhabu iumizayo.

وَ اِنْ لَّمْ يَنْتَهُوْا عَمَّا يَقُوْلُوْنَ لَيَمَسَّنَّ الَّذِيْنَ كَفَرُوْا مِنْهُمْ عَذَابٌ اَلِيْمٌ ﴿٧٣﴾

katika kila hali., na wameunganika kuwa Mungu mmoja na pia wamebaki kuwa watatu mbalimbali. Halmashauri ya Nicene na hasa *Athenacian Creed* (Itikadi ya Athenasi) ndio ya kwanza kutoa fundisho hili. Fundisho hilo ni itikadi kubwa ya dini ya Kikristo. Ah, tazama jinsi Wakristo walivyoanguka!

Wanasema, Mungu ni mmoja, lakini kwake wako nafsi tatu: Baba Mwana na Roho-Mtakatifu. Baba ni Mungu, Mwana ni Mungu na Roho Mtakatifu ni Mungu. Baba, na Mwana, na Roho-Mtakatifu si miungu watatu ni Mungu mmoja tu." (Katekisimu ya Katoliki, uk. 24). Huna haja ya kuyatazama sana maneno hayo ila utaona ya kuwa akili ya mtu ye yote haitapenda kuyakubali. Wachilia mbali shauri ya mshupavu. Maana yeye atakavyo, sawa au si sawa, hajali. Ni maneno ya "kisengele mbele, kisengele nyuma." Padre naye anayaona maneno hayo hayaelekei, ingawa ameyazoezwa toka utoto. Kujitoa ndani ya dhiki anatafuta kututosa ndani ya pango jingine la giza kwa kusema maneno hayo ni "Fumbo."

UTATU SI FUMBO.

Kusema ya kwamba utatu ni "fumbo" haikubaliki. Kusema, Baba ni Mungu, Mwana ni Mungu, Roho Mtakatifu ni Mungu, si maneno ya fumbo. Ni kukubali miungu watatu. Lakini kupinduka na kuwaambia watu ya kuwa hao miungu watatu si watatu bali ni mmoja, hayo tena si fumbo bali ni kuwachezea akili. Kama Petro ni mtu, Alois ni mtu, Yoan ni mtu, tunakubali, lakini akili ya mtu ye yote inakataa kusema hao watatu ni mtu mmoja. Kumwambia mtu asadiki ugali anaoula kuwa ni jiwe, na ya kuwa ni fumbo "tusiloweza kusikia barabara kwa akili zetu" siyo kumchezea na kumfanya juha? Kumwambia mtoto wa shule, 1 na 1na 1 ni moja, siyo kumdanganya? Hata kama ujipendekeze kwa kumwambia hilo ni fumbo, labda atakukubalia kwa kuwa hana haja ya ubishi zaidi, lakini akili yake haitakubali kuwa hilo ni fumbo. Atajua huo ni upumbavu: moja na moja na moja haiwezi kuwa moja. Akili inakataa. Fumbo halikataliwi na akili, bali akili hukubali kuwapo kwa fumbo na ikashindwa tu kujua ufumbuzi wake. Katika jambo la utatu, hakuna kushindwa kujua yasemwayo, ni neno lililo wazi kabisa kupotoka kwake hata akili inalihesabu kuwa ni kosa. Ni kama vile tunavyojua kitu hiki ni kizuri na hiki ni kibaya. Hakuna fumbo kamwe. Ni akili inakataa.

Mungu Baba asiwe mzee kuliko Mungu Mwana wake, na Mungu Mwana asiwe mdogo kuliko Mungu Baba yake, na Mungu Roho awe sawasawa na hao wawili. Je, ni maneno ya fumbo haya? Ni maneno wazi yanayoonyesha miungu watatu. Kila mmoja katika hao watatu binafsi yake ni Mungu "mwenye akili, aliye na uwezo wa kuchagua, na kutenda kitu, kwa kutaka mwenyewe peke yake." (Katekismu fungu 9). Sasa akili itakubali wapi kuwa hao watatu kila mmoja si Mungu wa peke yake? Kusema hili ni fumbo ni kupoteza wakati bure. Utatu si fumbo. Ni jambo lisilo na maana ambalo padre naye akili yake inaliona hivyo, na kwa kuwa amelizoezwa toka utoto na kwa bahati mbaya amefanikiwa kukuzoeza na wewe, hivyo lazima ajitetee hata kwa kiasi cha kukubali udhaifu wa imani hiyo kwa kuiita fumbo. Lakini si fumbo hilo. Hilo ni jambo tu linalokataliwa na akili kama vile inavyokataa mambo mengine yasiyo na maana.

MFANO ALIOELEZA PADRE HAUPATANI

Padre analeta mfano, na anasema, "Ni kama vile katika jua: katika jua mna jua lenyewe, ndicho kivimba chake, mna na anga lake, mna na moto wake. Vitu ni vitatu walakini jua ni moja. Basi kivimba cha jua, ni mfano wake Mungu Baba; anga lake, ndio mfano wa Mwana; na moto

wake, ndio mfano wa Roho-Mtakatifu." Tunamwuliza Bwana Padre: Je moto peke yake pasipo kivimba, unaweza kuitwa jua? Anga peke yake pasipo moto na pasipo kivimba linaweza kuitwa jua? Hivyo ni vitu vitatu vimeungana pamoja kufanya jua moja. Kimojapo kikikosekana, vilivyobaki havitaitwa jua, wala kilichoondoka kikiwa peke yake hakitaitwa jua. Lakini katika utatu kila nafsi peke yake ni Mungu mzima, ina akili, ina uwezo wa kuchagua na wa kutenda kitu, kwa kutaka yenyewe peke yake. Je vitu hivyo vitatu katika jua vikiwa mbalimbali, vinaweza kufanya kazi viifanyayo vinapokuwa pamoja? Kama mngalisema, zile nafsi tatu ni sehemu ndogo-ndogo za Mungu, ambazo kwa kuunganika zimefanya Mungu mmoja, hapo mfano wenu huu ungepatana. Lakini sasa ni kutafuta kucheza na maneno bure.

HOJA NYINGINE INAJIBIWA

Tena Padre ameleta mfano mwingine. "Ni kama vile rohoni mwa binadamu pana na kusikia, pana na kutaka, pana na kupenda, ndio mambo matatu mbalimbali, ijapokuwa roho ni moja," (uk. 25). Hapa maskini amejitosa ndani ya ujinga usiokadirika. Je, kusikia, kutaka, kupenda, hivi vitatu ndio roho moja? Kama ni hivyo, kuchukia, pia kuingizwe, kukataa pia kuingizwe, na mengineyo, na nafsi za roho zitakuwa zaidi kuliko tano. Je, kuna utano mtakatifu katika Uungu?

Bwana Padre anasema, "Sisi peke yetu, kwa akili zetu nzito, hatungaliweza kujua hayo, kwamba Mungu ni mmoja, mwenye nafsi tatu; walakini mwenyewe Mungu akawafumbulia watu." Mungu hawezi kuwaambia watu jambo la ujinga namna hii. Je, mnaweza kuonesha ni wapi katika Maagano ya Kale na Mapya palipoandikwa kuwa Mungu ana nafsi tatu, na kila nafsi peke yake ni Mungu kamili? Sasa kusema kuwa Mungu ndiye amefumbua jambo hilo, hali hakuna mahali po pote katika Vitabu vya Agano la Kale na Jipya palipoandikwa Mungu mmoja lakini nafsi tatu, maana yake ni nini? Kumsingizia Mungu? Wacheni kufuru zenu, na mwogopeni Allah. Msipoteze watu namna hii, na tubuni, au sivyo mtapasiwa hukumu iliyo kali kwa Allah.

YESU ANABATILISHA UTATU.

Yesu mwenyewe alisema, Baba ni mkubwa kuliko mimi (Yohana 14:28). Neno "mimi" alilosema Yesu, linaonyesha nafsi yake yeye mzima-mzima, ya kwamba ni mdogo kuliko Baba yake. Je, kuna Mungu mdogo na mkubwa? Sasa faida gani ya utatu? Tena Yesu alisema: Mtu anayemtukana Yesu atasamehewa, lakini anayesema maneno juu ya roho hatasamehewa. (Matt. 12:32).

Kusema kuwa Yesu ni Mungu, naye alikaa ndani ya tumbo la mwanamke kwa miezi tisa akila damu, akazaliwa wanavyozaliwa watoto wote, akalia, akanyonya, akalala, akaona njaa, akasali na kuomba Mungu, akakamatwa na maadui na kuteswa, na ya kwamba juu ya haya yote yeye ni Mungu, hakuna mtu ye yote atakayekubali hayo ila yule mwenye mawazo ya kipagani tu.

KATIKA AGANO LA KALE HAMNA UTATU

Kuna methali inayosema, "Anayezama, hushikilia hata kijiti." Wakristo waliposoma ndani ya Biblia Mungu anasema "Sisi" (Mwanzo 3:22), wakihimizwa na mawazo ya kipagani ya kuabudu miungu wengi yaliyoenea katika nchi zao, wakaona huu ndio msingi wa miungu watatu, Baba, Mwana na Roho. Lakini wanafunzi wa Nabii Musa na Manabii wa Kale, na sisi Waislamu tunajua kuwa neno hilo hutumika kwa kuonyesha heshima ya Mungu tu, na ushahidi ni kuwa Qur'an imetumia msemo huo mara kwa mara ingawa inalaumu kabisa imani ya utatu. Kadhalika neno "Sisi" siyo maana yake "Watatu," maana yake ni toka wawili mpaka idadi isiyojulikana. Mbona, tena, hawasemi kuwa nafsi za Mungu ni maelfu-elfu?

INJILI IMEVURUGIKA

Dalili nyingine wanayoleta juu ya utatu, ni aya mbili za kwanza za Injili ya Yohana. Hapo

75. Je, hawatubu kwa Allah na kumwomba msamaha? Na Allah ni Msamehevu, Mrehemevu.

اَفَلَا يَتُوْبُوْنَ اِلَى اللّٰهِ وَيَسْتَغْفِرُوْنَهٗ ؕ وَاللّٰهُ غَفُوْرٌ رَّحِيْمٌ ۝٧٤

76. Masihi bin Mariam siye ila ni Mtume tu; bila shaka Mitume wamekwisha fariki kabla yake; na mama yake ni mwanamke mkweli; wote wawili walikuwa wakila chakula. Tazama jinsi Tunavyowabainishia Aya, kisha tazama wanageuzwa wapi?

مَا الْمَسِيْحُ ابْنُ مَرْيَمَ اِلَّا رَسُوْلٌ ۚ قَدْ خَلَتْ مِنْ قَبْلِهِ الرُّسُلُ ؕ وَاُمُّهٗ صِدِّيْقَةٌ ؕ كَانَا يَاْكُلٰنِ الطَّعَامَ ؕ اُنْظُرْ كَيْفَ نُبَيِّنُ لَهُمُ الْاٰيٰتِ ثُمَّ انْظُرْ اَنّٰى يُؤْفَكُوْنَ ۝٧٥

---

imeandikwa, "Mwanzoni Neno alikuwako, na Neno alikuwa kwa Mungu, na Neno alikuwa ni Mungu. Huyo ndiye aliyekuwa kwa Mungu tangu mwanzo."

Soma maneno hayo mara mbili tatu, kisha ujiulize mwenyewe umefahamu nini? Wakristo wanasema Neno maana yake ni Yesu. Kama ni hivyo, Injili inasema, Mwanzoni Neno alikuwako, yaani mwanzoni Yesu alikuwako, na Mungu je? Hakuwa toka mwanzo? Tunajua Mungu ndiye awali na vyote vinamfuata. Injili hiyo inaonekana inapingana na Agano la Kale linalosema kuwa Mungu ndiye wa mwanzo (Isaya 44:6).Tena Yohana anaandika,"Na Neno alikuwa kwa Mungu," yaani Yesu alikuwa kwa Mungu. Hayo yanaonyesha kwamba Yesu na Mungu walikuwa pamoja, hakuna aliyemtangulia mwenziwe. Hivyo, haiwezekani Yesu awe mwana wa Mungu na Mungu kuwa baba yake, maana inabidi baba awe mbele kisha mwanawe amfuate. Ikiwa Yesu na Mungu walikuwa pamoja basi aitwe ndugu, asiitwe mwana, maana mwana hawezi kuwa marika ya babaye.

Kama 'Neno' maana yake pia ni Mungu, basi hapo maneno ya Injili yatasomeka hivi: - "mwanzoni Mungu alikuwako, na Mungu alikuwa kwa Mungu, na Mungu alikuwa ni Mungu." "Mungu alikuwa kwa Mungu," ni miungu wangapi basi? Mbona Wakristo wanasema "Tunamwamini Mungu Mmoja?" Kwa nini hawa miungu wengine wa siri hawawaondoi kabisa, abakie Mungu Mmoja wa Kweli?

MANENO YA YOHANA HAYAFAHAMIKI!

Labda Padre Dale atasema hii si tafsiri iliyo sahihi. Basi twamuliza, "Neno alikuwa kwa Mungu na Neno alikuwa ni Mungu" maana yake nini? Je, Mungu hajui kusema vizuri? "Alikuwa kwa Mungu" inaonyesha vitu viwili, na "Alikuwa ni Mungu" imebakisha kitu kimoja tu. Je, ni sawa kusema, "Mwanzoni kulikuwa kiti, na kiti kilikuwa kwa seremala, na kiti kilikuwa seremala?" au kusema, "Mwanzoni kulikuwa Petro, na Petro alikuwa kwa Yohana na Petro alikuwa Yohana?" Mtu mwungwana tu hatasema maneno yaliyo ovyo-ovyo kama hayo, sembuse Mungu!

Hata hivyo msomaji akumbuke ya kuwa maneno hayo ya Yohana, si ya Yesu. Yesu siye aliyesema; "Mwanzoni kulikuwa neno, na neno lilikuwa kwa Mungu na neno lilikuwa Mungu." Si Yesu aliyesema hivyo bali ni Yohana.Katika Injili zote Yesu hasemi, Mimi nilikuwa na Mungu mwanzoni, na mimi ndiye niliumba vitu vyote, kama wanavyodai leo Wakristo, bila kutoa shahada yo yote.

Injili ya Yoani iliandikwa miaka mingi baada ya kufa kwake Yesu. Inaonekana kwamba katika siku zilizoandikwa Injili hii Wakristo ndio ilikuwa mwanzo pole pole wanaanza kumpandisha Yesu daraja ya uungu. Imani ya utatu ilikuwa bado haijaanzwa, au sivyo tungemwona Roho-Mtakatifu amekwisha pachikwa katika aya hiyo, ili kuutimiza "Utatu Mtakatifu." Maneno ya Yohana hayataji nafsi tatu, bali anasema;"Huyu ndiye aliyekuwa kwa Mungu tangu mwanzo." Je Roho Mtakatifu alikuwa nani? Hakuna utatu basi!

77. Sema: Je, mnamwabudu badala ya Allah ambaye hawezi kuwadhuruni wala kuwafaidisheni? Na Allah ndiye Asikiaye, Ajuaye.

قُلْ اَتَعْبُدُوْنَ مِنْ دُوْنِ اللّٰهِ مَا لَا يَمْلِكُ لَكُمْ ضَرًّا وَّلَا نَفْعًا ؕ وَاللّٰهُ هُوَ السَّمِيْعُ الْعَلِيْمُ ﴿٧٦﴾

78. Sema: Enyi watu wa Kitabu! Msiruke mipaka ya dini yenu bila haki, wala msifuate matamanio ya watu waliokwisha potea toka zamani na wakawapoteza wengi, na wakaipotea njia iliyo sawa. ع

قُلْ يٰۤاَهْلَ الْكِتٰبِ لَا تَغْلُوْا فِيْ دِيْنِكُمْ غَيْرَ الْحَقِّ وَلَا تَتَّبِعُوْۤا اَهْوَآءَ قَوْمٍ قَدْ ضَلُّوْا مِنْ قَبْلُ وَاَضَلُّوْا كَثِيْرًا وَّضَلُّوْا عَنْ سَوَآءِ السَّبِيْلِ ﴿٧٧﴾ ع

FUNGU 11

79. Wamelaaniwa wale waliokufuru miongoni mwa wana wa Israeli kwa ulimi wa Daudi na wa Isa bin Mariam. Hayo ni kwa sababu waliasi nao walikuwa wakiruka mipaka.

لُعِنَ الَّذِيْنَ كَفَرُوْا مِنْ بَنِيْۤ اِسْرَآءِيْلَ عَلٰى لِسَانِ دَاوٗدَ وَعِيْسَى ابْنِ مَرْيَمَ ؕ ذٰلِكَ بِمَا عَصَوْا وَّكَانُوْا يَعْتَدُوْنَ ﴿٧٨﴾

80. Hawakuwa wenye kuzuiana mambo mabaya waliyoyafanya; bila shaka ni mabaya waliyokuwa wakiyafanya.

كَانُوْا لَا يَتَنَاهَوْنَ عَنْ مُّنْكَرٍ فَعَلُوْهُ ؕ لَبِئْسَ مَا كَانُوْا يَفْعَلُوْنَ ﴿٧٩﴾

Aya 78. *Msifuate matamanio ya watu waliokwisha potea toka zamani.* Maneno haya yanaonyesha ya kuwa fundisho la Utatu, Kafara ya damu ya Yesu, na Umwana wa Mungu ni mafundisho yaliyoazimwa, ambayo Wakristo waliyachukua kutoka kwa watu waliopotea zamani. Viongozi wa kwanza wa dini ya Kikristo walitia mabadilisho katika dini yao ili iwapendeze makabila ya kishenzi waliotaka kuwaingiza katika dini yao (1. Wakor. 9:19-23). Upelelezi wa siku hizi katika kutafuta chanzo cha Ukristo huu umehakikisha kabisa ukweli wa maneno ya Qur'an iliyotangaza miaka 1300 iliyopita kuwa Asili ya Ukristo wa leo ni upagani uliokuwa unashikwa na washenzi wa zamani, si mafundisho ya Bwana Yesu. (Soma Enc. Bib. , Col. 4695: Enc. R. Eth., vol. ii, p. 143: vol. vii, p. 436). Pia soma sura 9:30.

Aya 79. Katika Mitume wote wa Israeli, Daudi na Yesu ndio waliotaabishwa sana na Mayahudi. Yesu alipigiliwa msalabani na taabu za Daudi zinaonekana katika Zaburi zake. Laana ya Daudi ilifanya Waisraeli washambuliwe na Nebuchadnezzar (Bukhtanassar) ambaye aliuangamiza mji wa Jerusalem na akawachukua Mayahudi utumwani katika mwaka 586 B.C. Na laana ya Yesu iliwafanya washambuliwe na Titus aliyeiteka Jerusalem kama miaka 70 A.D. akavunja mji na kulinajisi Hekalu kwa kumchinja nguruwe humo, ambaye ni mnyama anayechukiwa na kuogopwa na Mayahudi.

تَرٰى كَثِيْرًا مِّنْهُمْ يَتَوَلَّوْنَ الَّذِيْنَ
كَفَرُوْا ؕ لَبِئْسَ مَا قَدَّمَتْ لَهُمْ اَنْفُسُهُمْ
اَنْ سَخِطَ اللّٰهُ عَلَيْهِمْ وَ فِي الْعَذَابِ
هُمْ خٰلِدُوْنَ ﴿٨١﴾

81. Utawaona wengi wao wanafanya urafiki na waliokufuru; kwa yakini ni mabaya ziliyowatangulizia nafsi zao: ya kwamba Allah Amewakasirikia, nao watakaa katika adhabu.

وَلَوْ كَانُوْا يُؤْمِنُوْنَ بِاللّٰهِ وَالنَّبِيِّ
وَمَاۤ اُنْزِلَ اِلَيْهِ مَا اتَّخَذُوْهُمْ اَوْلِيَآءَ
وَلٰكِنَّ كَثِيْرًا مِّنْهُمْ فٰسِقُوْنَ ﴿٨٢﴾

82. Na lau kama wangalimwamini Allah na Nabii na yaliyoteremshwa kwake, wasingaliwafanya hao kuwa marafiki; lakini wengi wao ni waasi.

لَتَجِدَنَّ اَشَدَّ النَّاسِ عَدَاوَةً لِّلَّذِيْنَ اٰمَنُوا
الْيَهُوْدَ وَالَّذِيْنَ اَشْرَكُوْا ۚ وَلَتَجِدَنَّ
اَقْرَبَهُمْ مَّوَدَّةً لِّلَّذِيْنَ اٰمَنُوا الَّذِيْنَ قَالُوْۤا
اِنَّا نَصٰرٰى ؕ ذٰلِكَ بِاَنَّ مِنْهُمْ قِسِّيْسِيْنَ
وَرُهْبَانًا وَّاَنَّهُمْ لَا يَسْتَكْبِرُوْنَ ﴿٨٣﴾

83. Hakika utawakuta walio maaduī zaidi kuliko watu (wengine) kwa waa minio ni Mayahudi na walio washirikina. Na utawaona walio karibu zaidi kwa urafiki na waaminio ni Wale wanaosema ya kuwa sisi ni Wakristo. Hayo ni kwa sababu wako miongoni mwao Makasisi na Maruhubani, na kwa sababu wao ha watakabari.

JUZU 7

وَاِذَا سَمِعُوْا مَاۤ اُنْزِلَ اِلَى الرَّسُوْلِ
تَرٰۤى اَعْيُنَهُمْ تَفِيْضُ مِنَ الدَّمْعِ مِمَّا
عَرَفُوْا مِنَ الْحَقِّ ۚ يَقُوْلُوْنَ رَبَّنَاۤ اٰمَنَّا
فَاكْتُبْنَا مَعَ الشّٰهِدِيْنَ ﴿٨٤﴾

84. Na wanaposikia yaliyoteremshwa kwa Mtume, utaona macho yao yakichuruzika machozi kwa sababu ya haki waliyoitambua; wanasema: Mola wetu tumeamini, basi utuandike pamoja na washuhudiao.

Aya 84. Hapa inaelezwa hali ya baadhi ya Wakristo waliokuwa siku za Mtume *s.a.w.*; na pia Aya hii inaeleza walivyo watu ambao nyoyo zao zinahangaika kutafuta haki na kuikubali po pote waionapo. Tena Aya hii inamhusu hasa mfalme Mkristo, Najashi wa nchi ya Abisinia. Jaafar bin ami wa Mtume *s.a.w.* pamoja na kikundi cha Waislamu waliokimbilia nchi hiyo, walitiliwa fitina kwa mfalme na Waarabu wa Makka waliokwenda kutaka kuwarudisha Makka kwa nguvu. Waarabu wale wakamwambia mfalme ya kuwa Waislamu hawamheshimu Masihi Yesu. Bwana Jaafar aliyekuwa ni msemaji wa Waislamu akamsomea mfalme Aya za kwanza za sura Mariam. Mfalme pamoja na rafiki zake walikuwa wakimwogopa Mungu wakaanza kulia waliposikia Aya zile. Mfalme Najashi akatamka kwa huruma sana akasema ya kuwa yeye pia anamwamini Yesu sawa kabisa na maneno yale na hamzidishii hata sawa na kijiti (Hisham jalada 1 uk. 305, 306).

وَمَا لَنَا لَا نُؤْمِنُ بِاللّٰهِ وَمَا جَآءَنَا مِنَ
الْحَقِّ ۙ وَنَطْمَعُ اَنْ يُّدْخِلَنَا رَبُّنَا مَعَ
الْقَوْمِ الصّٰلِحِيْنَ ﴿٨٥﴾

85. Na tuna nini tusimwamini Allah na haki iliyotufikia, na hali tunatumai ya kwamba Mola wetu Atatuingiza katika kundi la watu wema.

فَاَثَابَهُمُ اللّٰهُ بِمَا قَالُوْا جَنّٰتٍ تَجْرِيْ مِنْ
تَحْتِهَا الْاَنْهٰرُ خٰلِدِيْنَ فِيْهَا ؕ وَذٰلِكَ
جَزَآءُ الْمُحْسِنِيْنَ ﴿٨٦﴾

86. Basi Allah Akawalipa, kwa yale waliyoyasema, Bustani ipitayo mito ndani yake, humo watakaa milele. Na hayo ndio malipo ya wafanyao wema.

وَالَّذِيْنَ كَفَرُوْا وَكَذَّبُوْا بِاٰيٰتِنَآ اُولٰٓئِكَ
اَصْحٰبُ الْجَحِيْمِ ﴿٨٧﴾ ع

87. Na wale waliokufuru na kuzikadhibisha Aya Zetu, hao ndio watu wa Motoni.

FUNGU 12

يٰٓاَيُّهَا الَّذِيْنَ اٰمَنُوْا لَا تُحَرِّمُوْا طَيِّبٰتِ مَآ
اَحَلَّ اللّٰهُ لَكُمْ وَلَا تَعْتَدُوْا ؕ اِنَّ اللّٰهَ
لَا يُحِبُّ الْمُعْتَدِيْنَ ﴿٨٨﴾

88. Enyi mlioamini, msiharamishe vitu vizuri Alivyowahalalishieni Allah, wala msiruke mipaka. Hakika Allah Hawapendi warukao mipaka.

وَكُلُوْا مِمَّا رَزَقَكُمُ اللّٰهُ حَلٰلًا طَيِّبًا ۖ
وَّاتَّقُوا اللّٰهَ الَّذِيْٓ اَنْتُمْ بِهٖ مُؤْمِنُوْنَ ﴿٨٩﴾

89. Na kuleni katika vile Alivyokuruzukuni Allah vilivyo halali na vizuri; na Mcheni Allah Ambaye mnamwamini.

لَا يُؤَاخِذُكُمُ اللّٰهُ بِاللَّغْوِ فِيْٓ اَيْمَانِكُمْ
وَلٰكِنْ يُّؤَاخِذُكُمْ بِمَا عَقَّدْتُّمُ
الْاَيْمَانَ ۚ فَكَفَّارَتُهٗٓ اِطْعَامُ عَشَرَةِ
مَسٰكِيْنَ مِنْ اَوْسَطِ مَا تُطْعِمُوْنَ
اَهْلِيْكُمْ اَوْ كِسْوَتُهُمْ اَوْ تَحْرِيْرُ
رَقَبَةٍ ؕ فَمَنْ لَّمْ يَجِدْ فَصِيَامُ ثَلٰثَةِ
اَيَّامٍ ؕ ذٰلِكَ كَفَّارَةُ اَيْمَانِكُمْ اِذَا
حَلَفْتُمْ ؕ وَاحْفَظُوْٓا اَيْمَانَكُمْ ؕ كَذٰلِكَ
يُبَيِّنُ اللّٰهُ لَكُمْ اٰيٰتِهٖ لَعَلَّكُمْ
تَشْكُرُوْنَ ﴿٩٠﴾

90. Allah Hatawakamateni kwa viapo vyenu vya upuuzi, lakini Atawakamateni kwa viapo mlivyoviapa kwa nia. Basi kafara yake ni kuwalisha maskini kumi kwa kadiri ile mnayowalisha watu wa majumbani mwenu au kuwavisha, au kumpa uungwana mtumwa. Lakini asiyeweza kupata basi afunge saumu kwa siku tatu. Hii ndio kafara ya viapo vyenu mnapoapa; na vilindeni viapo vyenu. Hivyo ndivyo Allah Anavyowabainishieni Aya Zake ili mpate kushukuru.

Aya 88. Kama vile kuhalalisha kitu kilichoharimishwa ni kuvuka mipaka, kadhalika kuharimisha kitu kilichohalalishwa au kukiona kama ni haramu ni dhambi.

91. Enyi mlioamini! bila shaka vileo na kamari na masanamu (ya kuabudu) na mishale (ya ramli) ni uchafu wa kazi ya Shetani. Basi jiepusheni nayo, ili mpate kufaulu.

يٰٓاَيُّهَا الَّذِيْنَ اٰمَنُوْٓا اِنَّمَا الْخَمْرُ وَالْمَيْسِرُ وَالْاَنْصَابُ وَالْاَزْلَامُ رِجْسٌ مِّنْ عَمَلِ الشَّيْطٰنِ فَاجْتَنِبُوْهُ لَعَلَّكُمْ تُفْلِحُوْنَ ﴿٩١﴾

92. Hakika Shetani anataka tu kuunda uadui na bughudha kati yenu kwa (njia ya) vileo na kamari na kuwazuilieni kumkumbuka Allah na kusali. Basi je, mtaacha?

اِنَّمَا يُرِيْدُ الشَّيْطٰنُ اَنْ يُّوْقِعَ بَيْنَكُمُ الْعَدَاوَةَ وَالْبَغْضَآءَ فِى الْخَمْرِ وَالْمَيْسِرِ وَيَصُدَّكُمْ عَنْ ذِكْرِ اللّٰهِ وَعَنِ الصَّلٰوةِ ۚ فَهَلْ اَنْتُمْ مُّنْتَهُوْنَ ﴿٩٢﴾

93. Na mtiini Allah na mtiini Mtume na jihadharini. Lakini mkigeuka, basi jueni ya kwamba juu ya Mtume Wetu ni kufikisha tu (ujumbe) waziwazi.

وَاَطِيْعُوا اللّٰهَ وَاَطِيْعُوا الرَّسُوْلَ وَاحْذَرُوْا ۚ فَاِنْ تَوَلَّيْتُمْ فَاعْلَمُوْٓا اَنَّمَا عَلٰى رَسُوْلِنَا الْبَلٰغُ الْمُبِيْنُ ﴿٩٣﴾

94. Si dhambi juu ya waaminio na watendao mema kwa vile walivyovila endapo wakimcha (Mungu) na kuamini na kutenda mema, tena wakamcha (zaidi) na kuamini, tena wakamcha (zaidi) na kufanya hisani; na Allah Huwapenda wafanyao hisani.

لَيْسَ عَلَى الَّذِيْنَ اٰمَنُوْا وَعَمِلُوا الصّٰلِحٰتِ جُنَاحٌ فِيْمَا طَعِمُوْٓا اِذَا مَا اتَّقَوْا وَّاٰمَنُوْا وَعَمِلُوا الصّٰلِحٰتِ ثُمَّ اتَّقَوْا وَّاٰمَنُوْا ثُمَّ اتَّقَوْا وَّاَحْسَنُوْا ۗ وَاللّٰهُ يُحِبُّ الْمُحْسِنِيْنَ ﴿٩٤﴾ ع ١٢

Aya 91. *Pombe na kamari.* Miaka1300 imepita toka dini ya Kiislamu ilipoharamisha pombe na kamari. Injili za Wakristo hazisemi neno lo lote juu ya kamari ingawa ni kitu kibaya kabisa. Na kwa miaka mingi sana Wakristo wamejichezea kamari bila kusitasita. Lakini hivi karibuni kikundi cha Mapadre wapatao 16 walio ni wakubwa wa Makanisa mbalimbali ya dini ya Kikristo wametangaza maneno ya kulaumu kabisa michezo ya kamari na kusema ni kitu kibaya (*East African Standard,* July 17, uk. 5). Ni jambo la furaha ambalo linazidi kuhakikisha ya kuwa sharti mafundisho ya Kiislamu yafuatwe ndipo dunia itastawi. (pia tazama sura 2:174).

Aya 94. Siyo maana ya Aya hii kuwa mtu akiamini na kutenda wema anaweza kula chakula cha kila namna; bali Aya hii imeweka sharti ambayo mtu akiifuata atajiepusha na kula vyakula vilivyoharamishwa; yaani chakula kinachoweza kuleta dhara katika roho au mwili wa mtu. Na sharti yenyewe ni kwamba mtu amche Mungu na kuamini na kutenda mema; maana mwenye sifa hizi hawezi kamwe kufikiria kula vilivyoharamishwa. (Pia tazama sura 2:174)

FUNGU 13

95. Enyi mlioamini! bila shaka Allah Atawajaribuni kwa baadhi ya mawindo inayoyafikia mikono yenu na mikuki yenu, ili Allah Ajulishe ni nani anayemwogopa kwa siri; na atakayeruka mipaka baada ya hayo, basi yeye atapata adhabu iumizayo.

يَاَيُّهَا الَّذِيْنَ اٰمَنُوْا لَيَبْلُوَنَّكُمُ اللّٰهُ بِشَيْءٍ مِّنَ الصَّيْدِ تَنَالُهٗٓ اَيْدِيْكُمْ وَرِمَاحُكُمْ لِيَعْلَمَ اللّٰهُ مَنْ يَّخَافُهٗ بِالْغَيْبِ ۚ فَمَنِ اعْتَدٰى بَعْدَ ذٰلِكَ فَلَهٗ عَذَابٌ اَلِيْمٌ ﴿٩٥﴾

96. Enyi mlioamini! msiue mawindo na hali mmo katika Haji, na miongoni mwenu atakayemwua (mnyama) kwa kusudi, basi malipo yake yatakuwa sawa na alichokiua katika wanyama, kama watakavyohukumu waadilifu wawili miongoni mwenu, mnyama apelekwe katika Kaaba, au kutoa kafara kwa kuwalisha maskini au sawa na hayo ni kufunga saumu ili auonje ubaya wa jambo lake; Allah Amekwisha yasamehe yaliyopita; lakini atakayefanya tena Allah Atampa adhabu. Na Allah ndiye Mwenye ushindi kamili, Mwenye kuadhibu.

يَاَيُّهَا الَّذِيْنَ اٰمَنُوْا لَا تَقْتُلُوا الصَّيْدَ وَاَنْتُمْ حُرُمٌ ۭ وَمَنْ قَتَلَهٗ مِنْكُمْ مُّتَعَمِّدًا فَجَزَاۗءٌ مِّثْلُ مَا قَتَلَ مِنَ النَّعَمِ يَحْكُمُ بِهٖ ذَوَا عَدْلٍ مِّنْكُمْ هَدْيًۢا بٰلِغَ الْكَعْبَةِ اَوْ كَفَّارَةٌ طَعَامُ مَسٰكِيْنَ اَوْ عَدْلُ ذٰلِكَ صِيَامًا لِّيَذُوْقَ وَبَالَ اَمْرِهٖ ۭ عَفَا اللّٰهُ عَمَّا سَلَفَ ۭ وَمَنْ عَادَ فَيَنْتَقِمُ اللّٰهُ مِنْهُ ۭ وَاللّٰهُ عَزِيْزٌ ذُو انْتِقَامٍ ﴿٩٦﴾

97. Ninyi mmehalalishiwa mawindo ya bahari na chakula chake ndio posho yenu na kwa wasafiri; na mmeharamishiwa mawindo ya bara maadamu ninyi mmo katika hija; na Mcheni Allah Ambaye mtakusanywa Kwake.

اُحِلَّ لَكُمْ صَيْدُ الْبَحْرِ وَطَعَامُهٗ مَتَاعًا لَّكُمْ وَلِلسَّيَّارَةِ ۚ وَحُرِّمَ عَلَيْكُمْ صَيْدُ الْبَرِّ مَا دُمْتُمْ حُرُمًا ۭ وَاتَّقُوا اللّٰهَ الَّذِيْٓ اِلَيْهِ تُحْشَرُوْنَ ﴿٩٧﴾

Aya 97. Kwa kuwa kuwinda katika siku za Haji kunaweza kuleta udhia na hatari kwa ajili ya watu wengi wanaokwenda kwenye Kaaba, basi kumekatazwa. Lakini kuvua baharini kumeruhusiwa kwa sababu hakuleti udhia katika kusafiri watu.

جَعَلَ اللّٰهُ الْكَعْبَةَ الْبَيْتَ الْحَرَامَ
قِيٰمًا لِّلنَّاسِ وَالشَّهْرَ الْحَرَامَ وَالْهَدْيَ
وَالْقَلَآئِدَ ؕ ذٰلِكَ لِتَعْلَمُوْٓا اَنَّ اللّٰهَ يَعْلَمُ
مَا فِي السَّمٰوٰتِ وَمَا فِي الْاَرْضِ وَاَنَّ اللّٰهَ
بِكُلِّ شَيْءٍ عَلِيْمٌ ﴿٩٨﴾

98. Allah Ameifanya Kaaba, Nyumba tukufu, kuwa tegemeo la watu, na mwezi mtukufu na dhabihu na (wanyama wa dhabihu waliovishwa) makoja. Hayo ni kwa sababu mjue ya kwamba Allah Anayajua yaliyomo mbinguni na yaliyomo katika ardhi, na ya kwamba Allah ni mjuzi wa kila kitu.

اِعْلَمُوْٓا اَنَّ اللّٰهَ شَدِيْدُ الْعِقَابِ وَاَنَّ
اللّٰهَ غَفُوْرٌ رَّحِيْمٌ ﴿٩٩﴾ؕ

99. Jueni kwamba Allah ni Mkali wa kuadhibu, na ya kwamba Allah ni Msamehevu, Mrehemevu.

مَا عَلَى الرَّسُوْلِ اِلَّا الْبَلٰغُ ؕ وَاللّٰهُ يَعْلَمُ
مَا تُبْدُوْنَ وَمَا تَكْتُمُوْنَ ﴿١٠٠﴾

100. Si juu ya Mtume ila kufikisha tu, na Allah Anayajua mnayoyadhihirisha na mnayoyaficha.

قُلْ لَّا يَسْتَوِي الْخَبِيْثُ وَالطَّيِّبُ وَلَوْ
اَعْجَبَكَ كَثْرَةُ الْخَبِيْثِ ۚ فَاتَّقُوا اللّٰهَ
يٰٓاُولِي الْاَلْبَابِ لَعَلَّكُمْ تُفْلِحُوْنَ ﴿١٠١﴾ ع

101. Sema: Hauwi sawa ubaya na wema, ingawa wingi wa ubaya ukustaajabishe; basi Mcheni Allah, enyi wenye akili, ili mpate kufaulu.

FUNGU 14

يٰٓاَيُّهَا الَّذِيْنَ اٰمَنُوْا لَا تَسْـَٔلُوْا عَنْ اَشْيَآءَ
اِنْ تُبْدَ لَكُمْ تَسُؤْكُمْ ۚ وَاِنْ تَسْـَٔلُوْا عَنْهَا
حِيْنَ يُنَزَّلُ الْقُرْاٰنُ تُبْدَ لَكُمْ ؕ عَفَا اللّٰهُ
عَنْهَا ؕ وَاللّٰهُ غَفُوْرٌ حَلِيْمٌ ﴿١٠٢﴾

102. Enyi mlioamini! msiulize mambo ambayo mkidhihirishiwa yatawachukizeni. Na kama mtayauliza inapoteremshwa Qur'an mtayabainishiwa. Allah Ameyaacha hayo kutokana na huruma. Na Allah ni Msamehevu, Mvumilivu.

Aya 98. Haji ni tegemeo la watu katika manufaa ya dunia pia. Waislamu wa kila upande wanafika kwenye Kaaba na jambo hili linawapa msaada watu wa Makka. Nabii Ibrahimu alimwacha mkewe Hajira, pamoja na mwanawe, Ismail, katika jangwa la Paran karibu na Makka katika hali kama ya kuachwa wafe na njaa. Lakini Allah akatoa matumizi si kwa ajili ya Hajira na Ismail tu, bali pia kwa wazao wao wa baadaye. (Pia tazama sura 21:197 na 5:98).

Aya 101. Aya hii inaonya watu wasifuate wingi kama kipofu. Sifa ya kitu haijulikani kwa kuhesabu ni watu wangapi wanaokifuata, bali kina uzuri gani.

قَدْ سَاَلَهَا قَوْمٌ مِّنْ قَبْلِكُمْ ثُمَّ اَصْبَحُوْا بِهَا كٰفِرِيْنَ ﴿١٠٣﴾

103. Bila shaka watu wa kabla yenu waliyauliza, kisha wakawa wenye kuyakataa.

مَا جَعَلَ اللّٰهُ مِنْۢ بَحِيْرَةٍ وَّلَا سَآئِبَةٍ وَّلَا وَصِيْلَةٍ وَّلَا حَامٍ ۙ وَّلٰكِنَّ الَّذِيْنَ كَفَرُوْا يَفْتَرُوْنَ عَلَى اللّٰهِ الْكَذِبَ ؕ وَاَكْثَرُهُمْ لَا يَعْقِلُوْنَ ﴿١٠٤﴾

104. Allah Hakuagiza juu ya Bahiira wala Saaiba wala wasiila wala Haami; lakini wale waliokufuru wanamtungia uwongo Allah, na wengi wao hawatumii akili.

وَاِذَا قِيْلَ لَهُمْ تَعَالَوْا اِلٰى مَاۤ اَنْزَلَ اللّٰهُ وَاِلَى الرَّسُوْلِ قَالُوْا حَسْبُنَا مَا وَجَدْنَا عَلَيْهِ اٰبَآءَنَا ؕ اَوَلَوْ كَانَ اٰبَآؤُهُمْ لَا يَعْلَمُوْنَ شَيْـًٔا وَّلَا يَهْتَدُوْنَ ﴿١٠٥﴾

105. Na wanapoambiwa, njooni kwa Aliyoyateremsha Allah na kwa Mtume, husema: Yanatutosha yale tuliyowakuta nayo baba zetu. Je, hata kama baba zao walikuwa hawajui kitu wala hawakuongoka?

---

kiwezacho kukusudia kuwaletea matatizo. Hata hivyo kutokana na huruma Yake Allah Hapendi kutoa maagizo yakiwa yamefafanuliwa hata katika vijambo vidogo vidogo yasije yakawa magumu kwa baadhi ya watu kuyafuata na kusababisha usumbufu usiokuwa wa lazima.

Aya 104. *Bahiirah,* ni jina ambalo wapagani wa Kiarabu walimpa ngamia jike aliyezaa watoto saba na kisha akafunguliwa ili awe huru kwenda malishoni baada ya masikio yake kuchanwa. Ngamia huyu alitengwa kwa ajili ya matumizi ya mungu fulani na maziwa yake hayakuwa yakitumika wala mgongo wake.

Saaibah, ni ngamia jike aliyefunguliwa kwenda kwenye maji na malisho baada ya kuzaa watoto watano.

Waswiilah, ni ngamia jike (au kondoo jike au mbuzi jike) aliyefunguliwa kwa jina la mungu fulani baada ya kuzaa watoto saba wa kike mmoja baada ya mwingine. Iwapo katika mzao wake wa saba alizaa mapacha, dume na jike, hawa pia walifunguliwa.

Haami, ni ngamia aliyekuwa baba wa watoto saba. Hakufunguliwa na hakutumiwa kwa kupandwa au kubebea mizigo. Alikuwa huru kwenda kwenye malisho na kwenye maji.

Baada ya kusema kwamba mambo madogo madogo na ufafanuzi uliopita kiasi ameachiwa mtu mwenyewe kuyatungia sheria jinsi anavyofikiri kuwa ni sawa, aya hii kwa njia inayofaa kabisa inaelekeza uzingativu kwenye ukweli kwamba uhuru na hiari ya namna hiyo haviruhusiwi katika mambo ya msingi kwa sababu katika mambo ya msingi msimamo mmoja kwa watu wote ni jambo la lazima na mgawanyiko wa maoni waweza kuleta madhara makubwa sana. Aya hii inatupatia kielelezo chenye kuonesha kwamba akili ya binadamu haiwezi kukabidhiwa dhamana ya kutunga sheria za mambo ya msingi. Waarabu walikuwa wakiwafungulia wanyama waliotajwa katika aya hii kwa heshima ya masanamu yao. Licha ya msingi wake kuwa ukafiri na ushirikina, kitendo hiki pia kilikuwa ni cha upumbavu wa hali ya juu. Wanyama waliofunguliwa kwa namna hiyo walileta uharibifu mwingi sana kila walipokwenda. Qur'an inakirejea kitendo hiki kiovu kama mfano wa sheria zilizotungwa na binadamu na inawaonya Wakristo wanaohoji hekima iliyofunuliwa kujifunza somo kutokana na vitendo vyenye kushusha maadili mema ambavyo Waarabu wapagani walivikimbilia kwa sababu hawakuwa na sheria iliyofunuliwa ya kuwaongoza.

Aya 105. Tabia ya watu ni ya ajabu. Katika mambo ya kidunia wako tayari kuacha kila

يٰٓاَيُّهَا الَّذِيْنَ اٰمَنُوْا عَلَيْكُمْ اَنْفُسَكُمْ ۚ
لَا يَضُرُّكُمْ مَّنْ ضَلَّ اِذَا اهْتَدَيْتُمْ ۭ
اِلَى اللّٰهِ مَرْجِعُكُمْ جَمِيْعًا فَيُنَبِّئُكُمْ
بِمَا كُنْتُمْ تَعْمَلُوْنَ ﴿١٠٦﴾

106. Enyi mlioamini! Ninyi wenyewe ndio wenye kuwajibika na nafsi zenu. Hatawadhuruni aliyepotea ikiwa mko juu ya mwongozo. Marudio yenu nyote ni kwa Allah; basi Atawaambieni yale mliyokuwa mkiyatenda.

يٰٓاَيُّهَا الَّذِيْنَ اٰمَنُوْا شَهَادَةُ بَيْنِكُمْ اِذَا
حَضَرَ اَحَدَكُمُ الْمَوْتُ حِيْنَ الْوَصِيَّةِ
اثْنٰنِ ذَوَا عَدْلٍ مِّنْكُمْ اَوْ اٰخَرٰنِ
مِنْ غَيْرِكُمْ اِنْ اَنْتُمْ ضَرَبْتُمْ فِي
الْاَرْضِ فَاَصَابَتْكُمْ مُّصِيْبَةُ الْمَوْتِ ۭ
تَحْبِسُوْنَهُمَا مِنْۢ بَعْدِ الصَّلٰوةِ فَيُقْسِمٰنِ
بِاللّٰهِ اِنِ ارْتَبْتُمْ لَا نَشْتَرِيْ بِهٖ ثَمَنًا وَّلَوْ
كَانَ ذَا قُرْبٰى ۙ وَلَا نَكْتُمُ شَهَادَةَ اللّٰهِ اِنَّآ
اِذًا لَّمِنَ الْاٰثِمِيْنَ ﴿١٠٧﴾

107. Enyi mlioamini! muweke mashahidi wawili waadilifu miongoni mwenu, wakati wa kuusia, yanapomfikia mauti mmoja wenu, au wengine wawili wasiokuwa katika ninyi, mnapokuwa mkisafiri katika nchi na msiba wa mauti ukawafikieni. Mtawazuia hao wawili baada ya Sala, na waape kwa Allah, kama mkiwa na shaka, (wakisema): Hatutapokea thamani yo yote kwa haya ingawa ni jamaa (yetu), wala hatutaficha ushuhuda wa Allah; hakika hapo tutakuwa miongoni mwa wenye dhambi.

فَاِنْ عُثِرَ عَلٰٓى اَنَّهُمَا اسْتَحَقَّآ اِثْمًا
فَاٰخَرٰنِ يَقُوْمٰنِ مَقَامَهُمَا مِنَ الَّذِيْنَ
اسْتَحَقَّ عَلَيْهِمُ الْاَوْلَيٰنِ فَيُقْسِمٰنِ بِاللّٰهِ
لَشَهَادَتُنَآ اَحَقُّ مِنْ شَهَادَتِهِمَا وَمَا
اعْتَدَيْنَآ ۚ اِنَّآ اِذًا لَّمِنَ الظّٰلِمِيْنَ ﴿١٠٨﴾

108. Na kama ikijulikana ya kwamba hao wawili wamefanya dhambi, basi wawili wengine kutoka miongoni mwa wale ambao ushahidi umetolewa kinyume cha maslahi yao wasimame mahali pao. Kisha baada ya kula kiapo kwa jina la Allah watoe ushahidi dhidi ya wale wawili wa kwanza wakithibitisha; ushahidi wetu ni wa kweli zaidi kuliko ushahidi wa wale wawili wa kwanza na kwamba sisi hatukuruka mipaka waila hapo kwa hakika tutakuwa miongoni mwa wadhalimu.

---

upuuzi wanapoona mambo mapya ya ustaarabu. Lakini katika mambo ya dini ati hawataki kuacha ujinga waliowakuta nao baba zao!

Aya 107. *Au wengine wawili.* Kadhi maarufu Shuraih, anasema ya kuwa katika hali ya safari mambo ya wasia yanaweza kushuhudiwa hata na watu wasio Waislamu.

ذٰلِكَ اَدۡنٰۤى اَنۡ يَّاۡتُوۡا بِالشَّهَادَةِ عَلٰى وَجۡهِهَاۤ اَوۡ يَخَافُوۡۤا اَنۡ تُرَدَّ اَيۡمَانٌۢ بَعۡدَ اَيۡمَانِهِمۡ ؕ وَاتَّقُوا اللّٰهَ وَاسۡمَعُوۡا ؕ وَاللّٰهُ لَا يَهۡدِى الۡقَوۡمَ الۡفٰسِقِيۡنَ ﴿۱۰۹﴾ ع

109. Hiyo inaelekea zaidi ya kwamba watoe ushahidi kama ulivyo au wahofie visije vikaletwa viapo vingine baada ya viapo vyao. Na mcheni Allah na sikieni; na Allah Hawaongozi watu waasi.

FUNGU 15

يَوۡمَ يَجۡمَعُ اللّٰهُ الرُّسُلَ فَيَقُوۡلُ مَاذَاۤ اُجِبۡتُمۡ ؕ قَالُوۡا لَا عِلۡمَ لَنَا ؕ اِنَّكَ اَنۡتَ عَلَّامُ الۡغُيُوۡبِ ﴿۱۱۰﴾

110. Siku ambayo Allah Atawakusanya Mitume na Atasema: Mlijibiwa nini? Watasema: Hatujui, bila shaka Wewe ndiye Ujuaye sana mambo ya siri.

اِذۡ قَالَ اللّٰهُ يٰعِيۡسَى ابۡنَ مَرۡيَمَ اذۡكُرۡ نِعۡمَتِىۡ عَلَيۡكَ وَعَلٰى وَالِدَتِكَ ۘ اِذۡ اَيَّدتُّكَ بِرُوۡحِ الۡقُدُسِ ۟ تُكَلِّمُ النَّاسَ فِى الۡمَهۡدِ وَكَهۡلًا ۚ وَاِذۡ عَلَّمۡتُكَ الۡكِتٰبَ وَالۡحِكۡمَةَ وَالتَّوۡرٰىةَ وَالۡاِنۡجِيۡلَ ۚ وَاِذۡ تَخۡلُقُ مِنَ الطِّيۡنِ كَهَيۡـَٔةِ الطَّيۡرِ بِاِذۡنِىۡ فَتَنۡفُخُ فِيۡهَا فَتَكُوۡنُ طَيۡرًا بِاِذۡنِىۡ وَتُبۡرِئُ الۡاَكۡمَهَ وَالۡاَبۡرَصَ بِاِذۡنِىۡ ۚ وَاِذۡ تُخۡرِجُ الۡمَوۡتٰى بِاِذۡنِىۡ ۚ وَاِذۡ كَفَفۡتُ بَنِىۡۤ اِسۡرَآءِيۡلَ عَنۡكَ اِذۡ جِئۡتَهُمۡ بِالۡبَيِّنٰتِ فَقَالَ الَّذِيۡنَ كَفَرُوۡا مِنۡهُمۡ اِنۡ هٰذَاۤ اِلَّا سِحۡرٌ مُّبِيۡنٌ ﴿۱۱۱﴾

111. Allah Atakaposema: Ewe Isa mwana wa Mariam, kumbuka neema yangu juu yako na juu ya mama yako; Nilipokusaidia kwa maneno matakatifu, ukazungumza na watu utotoni na katika utu uzima na Nilipokufundisha Kitabu na hekima na Taurati na Injili na ulipotengeneza kwa udongo sawa na matengenezo ya ndege, kwa idhini Yangu, kisha ukapulizia, ndipo akawa ndege kwa idhini Yangu; na ulipowaponya vipofu na wenye ukoma kwa idhini Yangu, na ulipowatoa wafu kwa idhini Yangu, na Nilipokuzuilia wana wa Israeli ulipowafikia kwa Ishara zilizo wazi, ndipo wale waliokufuru miongoni mwao wakasema: Haya si cho chote ila ni udanganyifu dhahiri.

Aya 111. *Ukazungumza na watu utotoni na katika utu uzima;* Huu ni usemi unaoonyesha kwamba Yesu alizungumza maneno ya hekima na ya kiucha-Mungu tangu siku za mwanzo za utoto wake na aliendelea kufanya hivyo hata alipokuwa amefikia umri wa uzee Neno

وَاِذْ اَوْحَيْتُ اِلَى الْحَوَارِيّٖنَ اَنْ اٰمِنُوْا بِيْ وَبِرَسُوْلِيْ ۚ قَالُوْٓا اٰمَنَّا وَاشْهَدْ بِاَنَّنَا مُسْلِمُوْنَ ﴿١١٢﴾

112. Na Nilipowafunulia wanafunzi kwamba Niaminini Mimi na Mtume Wangu, wakasema: Tumeamini na Uwe shahidi ya kwamba sisi ni wanyenyekevu.

اِذْ قَالَ الْحَوَارِيُّوْنَ يٰعِيْسَى ابْنَ مَرْيَمَ هَلْ يَسْتَطِيْعُ رَبُّكَ اَنْ يُّنَزِّلَ عَلَيْنَا مَآئِدَةً مِّنَ السَّمَآءِ ؕ قَالَ اتَّقُوا اللّٰهَ اِنْ كُنْتُمْ مُّؤْمِنِيْنَ ﴿١١٣﴾

113. Wanafunzi waliposema: Ewe Isa mwana wa Mariamu, je, Mola wako Anaweza kututeremshia chakula kutoka mbinguni? Akasema: Mcheni Allah kama ninyi ni waaminio.

قَالُوْا نُرِيْدُ اَنْ نَّاْكُلَ مِنْهَا وَتَطْمَئِنَّ قُلُوْبُنَا وَنَعْلَمَ اَنْ قَدْ صَدَقْتَنَا وَنَكُوْنَ عَلَيْهَا مِنَ الشّٰهِدِيْنَ ﴿١١٤﴾

114. Wakasema: Tunataka kula katika hicho na ili mioyo yetu itulie na tujue ya kwamba umetuambia kweli na tuwe juu ya hayo miongoni mwa wanaoshuhudia.

قَالَ عِيْسَى ابْنُ مَرْيَمَ اللّٰهُمَّ رَبَّنَآ اَنْزِلْ عَلَيْنَا مَآئِدَةً مِّنَ السَّمَآءِ تَكُوْنُ لَنَا عِيْدًا لِّاَوَّلِنَا وَاٰخِرِنَا وَاٰيَةً مِّنْكَ ۚ وَارْزُقْنَا وَاَنْتَ خَيْرُ الرّٰزِقِيْنَ ﴿١١٥﴾

115. Akasema Isa bin Mariam: Ee Allah, Mola wetu, tuteremshie chakula kutoka mbinguni ili kiwe sikukuu kwa ajili ya wa mwanzo wetu na wa mwisho wetu, na kiwe Ishara itokayo Kwako, na Uturuzuku, kwani Wewe ni Mbora wa wanaoruzuku.

kahlan linaonyesha ule wakati ambapo nywele za mtu zinageuka na kuanza kuwa za kijivujivu na kuanzia hapo hadi kufikia umri wa uzee.

Aya hii ni msemo wa kimethali wa mapinduzi ya kiroho yaliyoletwa na manabii wa Allah. Hii ni sifa maalumu ya tabia njema za Yesu ambaye kati ya Manabii wote wa Allah aliteuliwa kama mfano wa kuleta mageuzi ya kimiujiza kama hayo.

Nilipokuzuilia wana wa Isaraeli, yaani walizuiliwa wasiweze kumwua Yesu. Habari nyingine za Aya hii tazama sura 2:57; 2:88; 2:254; 3:47; 3:50; 3:60 na 4:158. Pia ikumbukwe ya kuwa Mtume Muhammad s.a.w. aliahidiwa kulindwa na akalindwa, na maadui wake wasiweze kumdhuru walivyokusudia. Maadui wa Mtume s.a.w. walizuiwa wasiweze kumwua kama ilivyoahidiwa katika sura 5:68. Uadui wa Makka, hatari za Madina, kujeruhiwa katika vita vya Uhud na alipobaki peke yake katika vita vya Hunain akirushiwa mishale kama mvua, mote humo na mwinginemo alisalimika na baadaye akafa kifo cha kawaida. Kutimia kwa ahadi hii ya Allah kuko wazi kabisa.

Aya 115. *Maaidatam-minassamaai,* "Chakula kutoka mbinguni." Maneno haya yanaonyesha ya kuwa wanafunzi wa Nabii Isa hawakuomba chakula cha mara moja bali chakula kisichokwisha kinachopatikana bila taabu. Aya hizi siyo mradi wao ya kuwa chakula kiliteremka kutoka mbinguni, maana si desturi ya Allah kuonyesha miujiza ya namna hii, kwani mtu ye yote hangeweza kuikataa kwa vile ni jambo la ajabu kuona chakula kushuka toka mbinguni. (Tazama malinganisho, sura 1:6).

قَالَ اللّٰهُ اِنِّیۡ مُنَزِّلُهَا عَلَیۡکُمۡ ۚ فَمَنۡ یَّکۡفُرۡ بَعۡدُ مِنۡکُمۡ فَاِنِّیۡۤ اُعَذِّبُهٗ عَذَابًا لَّاۤ اُعَذِّبُهٗۤ اَحَدًا مِّنَ الۡعٰلَمِیۡنَ ﴿۱۱۵﴾

116. Allah Akasema: Bila shaka Mimi Nitakiteremsha juu yenu, lakini miongoni mwenu atakayekataa baada ya haya, basi Mimi Nitamwadhibu adhabu ambayo Sijamwadhibu ye yote katika walimwengu.

FUNGU 16

وَاِذۡ قَالَ اللّٰهُ یٰعِیۡسَی ابۡنَ مَرۡیَمَ ءَاَنۡتَ قُلۡتَ لِلنَّاسِ اتَّخِذُوۡنِیۡ وَاُمِّیَ اِلٰهَیۡنِ مِنۡ دُوۡنِ اللّٰهِ ؕ قَالَ سُبۡحٰنَکَ مَا یَکُوۡنُ لِیۡۤ اَنۡ اَقُوۡلَ مَا لَیۡسَ لِیۡ ۟ بِحَقٍّ ؕ اِنۡ کُنۡتُ قُلۡتُهٗ فَقَدۡ عَلِمۡتَهٗ ؕ تَعۡلَمُ مَا فِیۡ نَفۡسِیۡ وَلَاۤ اَعۡلَمُ مَا فِیۡ نَفۡسِکَ ؕ اِنَّکَ اَنۡتَ عَلَّامُ الۡغُیُوۡبِ ﴿۱۱۶﴾

117. Na Allah Atakaposema: Ewe Isa bin Mariam! je, wewe uliwaambia watu: Nishikeni mimi na mama yangu kuwa miungu wawili badala ya Allah? Atasema: Wewe ndiwe Mtakatifu, hainipasi mimi kusema ambayo sina haki (ya kusema); kama ningalisema bila shaka Ungalijua; Unayajua yaliyomo nafsini mwangu, lakini mimi siyajui yaliyomo nafsini Mwako; hakika wewe ndiwe Ujuaye sana mambo ya ghaibu.

Aya 116. Aya hii inaonyesha ya kuwa Allah alikubali kuwapa Wakristo chakula kingi, na akawapa, kwa sharti ya kuwa wakiacha kuamini adhabu kali mno itawashukia. Baadaye Wakristo wakaacha imani na adhabu waliyoiogofya imekwisha shuka. Vita mbili zilizopita pamoja na matokeo yake yasiyotazamiwa ndio sura moja ya kutimia bishara hii ya ajabu, na Allah ndiye ajuaye baadaye bishara hii itaendelea kujileta kwa sura gani za kutisha, na misiba gani mizito inayowangojea Wakristo katika dunia hii na Akhera.

Aya 117. Siku ya Kiyama Allah atamleta Yesu kuwasuta Wakristo ambao hata leo wanamwabudu Yesu na kumpa daraja ya uungu. Kadhalika mama yake wanamwita "malkia wa Mbinguni" na ya kuwa hakufa, alipaa mbinguni mzima; na daima wanamwomba. Padre Dale anasema, "Hapana Mkristo asadikiye ya kuwa Bwana wetu alimwita mama yake, Mungu, wala hapana Mkristo aaminiye ya kuwa Bwana wetu alidai kuwa Mungu wa pili. Kama Muhammad angalifahamu dini yetu asingalisema haya." (Uk. 587 wa Tafsiri yake.).

Sisi tunashangaa sana kuona Padre mzima anaweza kuonesha ujahili wa kiasi hiki. Je, Aya hii inasema kuwa Yesu alimwita mama yake Mungu? Au je, Aya inasema kuwa Yesu alijiita Mungu wa pili? Aya haisemi hivyo. Aya inaonyesha waziwazi ya kuwa Allah atamwuliza Yesu juu ya imani ya Wakristo waliyoshika baadaye ya kumwabudu yeye na mama yake. Kuelekeza sala kwa kitu cho chote ni kukiabudu. Masanamu ya Yesu na Mariamu maelfu elfu yamesimamishwa, na hawa wote wawili wanaombwa, na hivyo wanafahamiwa kuwa miungu. Mungu atamwuliza Yesu, je, wewe uliwaambia hawa wakuabudu wewe na mamaako? Kisha Allah anaonyesha ya kuwa Yesu atakataa na kusema hana habari ya mambo yaliyotokea nyuma yake. Hivyo uwongo wa Wakristo kumsingizia Yesu kujidai uungu, na kumtukuza mama yake kama Malkia wa mbinguni na mama wa Mungu, utawafedhehi. Allah anajua Yesu hakuwaambia Wakristo wapotee hivyo, lakini kuwahakikishia dhambi yao,

Yesu ataitwa kutoa ushahidi wake.

Mahali pengine Allah amesema, siku ya Kiyama mashahidi wataletwa toka kila umati kutoa ushahidi wao juu ya wakosefu katika nyimati zao. Mashahidi hao ni Manabii. Manabii hawatahukumiwa, bali wataletwa kuwasuta watu waovu.

Padre Dale, hakuweza kufahamu maana hii, akaandika, "Yaani Bwana wetu atatoa hesabu siku ya mwisho kama watu wengine (uk. 586-587 wa Tafsiri yake). Na mbele amesema, "Lakini sisi tunasadiki ya kuwa (Yesu) ndiye atakaemhukumu Muhammad."

Hapa hasira yake na ghadhabu yake inaonekana waziwazi. Kwanza hakufahamu maana ya Aya hiyo ni nini, akadhani Mitume wote watahukumiwa. Kusema ya kwamba Yesu atamhukumu Muhammad ni maneno ya uchokozi yasiyo na dalili yo yote.

YESU SI HAKIMU

Je, Yesu alikuja kuhukumu? Yesu mwenyewe anasema, "Maana Mungu hakumpeleka Mwana wake ulimwenguni auhukumu ulimwengu bali ulimwengu uokolewe naye" (Yohana 3:17). Maneno haya yanaonyesha wazi kuwa Yesu hakuja kuhukumu. Na hata kama yaletwe maneno katika Injili yasemayo Yesu alikuja hukumu, yatakuwa ni maneno ya bure tu. Yeye ndiye alihukumiwa. Alishikwa, akapelekwa kortini, japo alikuwa hana kosa hakuweza kujisaidia, akakatiwa hukumu ya kuuawa, akatundikwa mtini; wanafunzi wake wakamkimbia wasiweze kumsaidia; yeye mwenyewe naye asiweze kujisaidia, akapiga kelele kulia, "Mungu wangu, Mungu wangu mbona umeniacha?" (Mat. 27:46). Je, mtu wa namna hiyo anaweza kusemwa alikuja hukumu, na mtu mwenye akili yake akakubali? Kama hakuweza kuhukumu hata adui yake mmoja hapo kwanza, atawezaje baadaye?

Yesu alisema, "Amini, amin, nawaambieni, Alisikiaye neno langu na kumwamini yeye aliyenipeleka ana uzima wa milele, wala hafiki hukumuni, bali amepita toka mauti hata uzima" (Yohana 5:24). Waislamu wote wamefundishwa na Mtume Muhammad *s.a.w.* kumwamini Mungu aliyemtuma Yesu, wamefundishwa kuamini Malaika, na Mitume na Vitabu na Uwezo wa Allah na siku ya Kiyama. Zaidi ya hayo dini ya Kiislamu imemfadhili sana Yesu. Kama si Mtume Muhammada *s.a.w.* hakuna hata Mwislamu mmoja angaliamini kuwa Yesu alizaliwa bila baba. Kama si Mtume Muhammad *s.a.w.* Waislamu wote wangekubali kuwa Yesu amelaaniwa kwa kufishwa msalabani. Yesu hangeweza kumhukumu Muhammad. Mtume Muhammad *s.a.w.* alisema, "Kama Musa na Isa wangekuwa hai wasingekuwa na njia ila kunifuata" (Al-Yawakit, Jalada 2, uk. 22). Yesu mbele ya Mtume Muhammad *s.a.w.* ni kama mwanafunzi tu. Mtume Muhammad *s.a.w.* alisema, "Wanazuoni wa umati wangu ni kama Manabii wa wana wa Israeli." Lakini ingawa Mtume Muhammad *s.a.w.* ni mkubwa kabisa namna hii, ambaye alishinda adui zake, na uwezo wa Mungu ukadhihirika kabisa katika dhati yake, sisi Waislamu hatusemi kuwa yeye atamhukumu Yesu. Manabii na watu wasio na kosa hawawezi kuhukumiwa kama alivyokwisha bainisha hata Yesu mwenyewe hapo juu. Basi Mkristo, asipoacha Injili yake, hawezi kusema kwamba Waislamu, wanaomuamini Mungu yule yule anayeaminiwa na Yesu, wanaweza kuhukumiwa na Yesu.

Siku ya Kiyama Mungu Mwenyezi atawahukumu wenye dhambi. Yesu atakuwa chini ya amri ya Mungu. Paulo anasema, "Basi, vitu vyote vikiisha kutiishwa chini yake, ndipo Mwana mwenyewe naye atatiishwa chini yake aliyemtiishia vitu vyote, ili Mungu awe yote katika yote." (1 Wakor. 15:28).

Hakika ni hiyo iliyokwisha elezwa hapo juu kwamba Nabii Isa atawafedhehesha wafuasi wake waovu kwa kukana imani yao. Katika Injili hizi yamo maneno yanayosadikisha hayo. Yesu alisema, "Wengi wataniambia siku ile, Bwana, hatukufanya unabii kwa jina lako, na kwa jina lako kufukuza pepo, na kwa jina lako kufanya miujiza mingi? Ndipo nitawaambia dhahiri, Sikuwafahamu ninyi wakati wo wote: ondokeni kwangu, ninyi mtendao maovu" (Matt. 7:22-23). Basi watakaofukuzwa siku ya Kiyama kwa ushahidia wa Yesu ni wale tu wanaomwita, Bwana, Bwana; si watu wote. Wakristo nawaangalie vizuri maneno hayo.

KWA NINI YESU ATAWAFUKUZA WAKRISTO.

Sababu za kufukuzwa kwa Wakristo siku ya Kiyama ni nyingi, lakini iliyo kubwa ni udhaifu wa imani yao kwa Allah. Yesu aliwaita wafuasi wake, "wenye imani haba" na "Kizazi kipotofu" (Matt. 16:8 na 17:17, 20). Na baada ya kufariki kwake walimsingizia mambo mabaya mengi ajabu. Walisema, Alitengeneza ulevi (Yohana 2:1-11). Walisema alikaa na shetani (Luka 4:12, 13. Walisema kwamba alilaaniwa (Wagalatia 3:13) na akaenda Jahanamu (1 Petro 3:19, Matendo 2:31); kwamba alimkaripia mama yake (Yohana 2:4); kwamba alimwita mwanamke mmoja "mbwa" (Matt. 15:26), kwamba watu waliomwomba awaonyeshe ishara akawatukana kuwa ni watoto wa zinaa (Matt. 12:39), kwamba akamwita mwanafunzi wake Petro, "Shetani" (Mat. 16:23). Alimwahidi mwizi mmoja aliyetundikwa naye msalabani siku ile kuwa wote wawili wataiangia peponi (Luka 23:43), lakini tena yeye mwenyewe akashuka ndani ya Jahanamu (1 Petro 3:19, Matendo 2:31); ya kwamba Manabii wote waliomtangulia aliwaita wezi na wanyang'anyi (Yohana 10:8), na ya kwamba hata yeye mwenyewe hakutaka kuitwa mwema (Luka 18:19).

NA MUNGU WAMEMSINGIZIA.

Allah naye wamemsingizia. Wanasema Mungu baada ya kufanya kazi kwa siku sita, siku ya saba akapumzika (Mwanzo 2:2). Ndio kusema alichoka, maana hapumziki ila yule anayeshikwa na mchoko. Kama Mungu anachoka, basi naye ni dhaifu? Haiwezekani. Hapa Mungu amedhalilishwa. Isitoshe, Mungu amesingiziwa kwamba alimwambia Nabii Wake, Daudi, "Mimi hapa nitakuinulia wewe uovu juu yako katika nyumba yako mwenyewe, nami nitawatwaa, hao wakezo mbele ya macho yako, nami nitampa jirani yako, naye, atalala na wakezo katika nuru ya jua hili" (2 Samuel 12:11). Je, kazi hii ya Shetani kunasibishwa na Mungu, siyo kumsingizia?

MALAIKA WAMESINGIZIWA

Malaika nao hawakubakishwa na jamaa hao, nao pia wamelaumiwa. Wanasema ya kuwa Shetani na Malaika wamewekewa moto wa milele (Matt. 25:41); ya kwamba Malaika nao walikosa, Mungu akawatupa shimoni, akawatia katika mafungo ya giza (2 Petro 2:4; Yuda 1:6). Qur'an inatufundisha kuwa Malaika hawamwasi Mungu na wanatenda yote wanayoamrishwa (sura 66:7).

MANABII WAMESINGIZIWA

Manabii nao wamepewa aibu: Nabii Nuhu anasemwa alilewa, akafuama, (Mwanzo 9:20-21); Nabii Luti anasemwa binti zake walimlewesha mvinyo, usiku wakawa wakienda lala naye siku kwa siku, akawatia mimba wakazaa (Mwanzo 19:30-38); ya kwamba, mtoto wa Nabii Yakubu, aitwaye Ruben, alilala na mama yake aliyekuwa suria wa baba yake, Nabii Yakubu (Mwanzo 35:22); ya kwamba Nabii Musa aliua mtu kusudi, alimkuta mtu huyo anagombana na nduguye. Musa akaangalia huku na huku, alipoona hakuna mtu, akamwua yule mtu na akamficha ndani ya mchanga (Kutoka 2:12); ya kwamba Nabii Harun alifanyiza mungu wa sanamu ya ndama, na akawakusanya Waisraeli kuabudu sanamu hilo (Kutoka 32:2-6); ya kwamba Nabii Daudi alimtamani mwanamke mzuri aliyekuwa mke wa mtu aitwaye Uria, akamchukua yule bibi na kumwulisha mumewe kwa kumpeleka vitani (2 Samuel 11:2-5; 14-17); ya kwamba Nabii Sulemani alipenda sana wanawake wa kikafiri ambao baadaye wakamfanya murtadi, akaingia dini yao na kuabudu miungu ya uwongo na kuwajengea miungu hao mahali pa kuabudiwa (1 Wafalme 11:1-8).

Yote hayo ndio fikira za Wakristo juu ya Allah, Malaika Wake, Manabii Wake, na hata Yesu hakupona na kuaibishwa huko. Ilikuwa lazima afike Mtume Muhammad *s.a.w.* pamoja na Qur'an ili kusahihisha makosa yao. Lakini, naye pia wamempindukia kwa maneno

مَا قُلْتُ لَهُمْ اِلَّا مَآ اَمَرْتَنِيْ بِهٖٓ اَنِ اعْبُدُوا اللّٰهَ رَبِّيْ وَرَبَّكُمْ ۚ وَكُنْتُ عَلَيْهِمْ شَهِيْدًا مَّا دُمْتُ فِيْهِمْ ۚ فَلَمَّا تَوَفَّيْتَنِيْ كُنْتَ اَنْتَ الرَّقِيْبَ عَلَيْهِمْ ۭ وَاَنْتَ عَلٰي كُلِّ شَيْءٍ شَهِيْدٌ ۝۱۱۷

118. Sikuwaambia lo lote ila yale Uliyoniamuru: ya kwamba Mwabuduni Allah, Mola wangu na Mola wenu; na nilikuwa shahidi juu yao nilipokuwa kati yao, lakini Uliponifisha Wewe Ukawa Mchungaji juu yao, na Wewe ni Shahidi juu ya kila kitu.

---

kama yale wanayowatwika nayo Manabii waliomtangulia, na mengi yasiyostahili wameandika kumsingizia. Soma Katekisimu ya Katoliki iliyotangazwa na Catholic Bookshop, P. O. Box 891, Nairobi, uk. 84-85; na Ukweli uko wapi? mlango 11.

MTUME MUHAMMAD s.a.w. ANASINGIZIWA

Ingawa Mtume *s.a.w.* hakujua kusoma wala kuandika, lakini Katekisimu hiyo inasema, "Hata siku moja akatoka mjini, akaenda zake mbali, akajificha katika pango la Hira, akakaa kule siku nyingi, akiandika dini mpya. Alipokwisha kazi hiyo ya kuandika, akaondoka pangoni, akarudi kwa watu wake," Wanasema, Mtume *s.a.w.* "alikuwa hawezi kifafa." Na maneno mengi ya matusi na uwongo yameandikwa katika vitabu mbalimbali vya Wakristo. Na kwao wao washenzi ni nani? Wanasema, "Washenzi ndio watu wasiobatizwa, wasiomjua Mungu, au waliomjua kidogo tu, kama watu wa bara hii, *kama Waislamu* . . . . " (Katekisimu uk. 84).

Hayo yote ni uwongo. Kwa hiyo Yesu atawakana mbele ya Allah. Wakristo wangempenda Yesu wangemhishimu sana Mtume Muhammad *s.a.w.* Maana yeye alimtukuza Yesu katika masingizio yote. Injili mapaka sasa inaonyesha kuwa kulikuwa maneno mengine ya Yesu yalikuwa uwongo, ya kwamba alikuwa mnywaji wa mvinyo, mtukanaji, mlaaniwa, na mtu asiye na wema wo wote. Mtume Muhammad *s.a.w*. alimtakasa na kumwokoa na maneno hayo machafu, na katika Qur'an pia Yesu akatajwa kuwa yu mtu mwema, mtakatifu, Nabii Mtukufu aliyesaidiwa na Roho Takatifu. Hata mama yake alipewa heshima impasayo katika Qur'an. Je, kwa sababu ya ihsani hii Padre Dale na wenzake wanamchukia Mtume wa Uislamu pasina haki? Yesu aliwaagiza wafuasi wake, akisema, "Mimi nawaambieni. Wapendeni adui zenu, wabarikini wanaowalaani" (Matt. 5: 44). Lakini hao mapadre ni wafuasi wa nani ambao wanamchukia aliyewatendea wema na kumlaani aliyewaita kwenye mwongozo? Je, Mtume Muhammad analaumiwa kwa sababu ya "dhambi" ya kumsifu Yesu?

Aya 118. *Uliponifisha Wewe Ukawa Mchungaji wao.* Neno *tawaffaitanii* "Uliponifisha" limetumiwa na Mtume *s.a.w.* aliposema, "Siku ya Kiyama baadhi ya watu wa umati wangu watapelekwa upande wangu wa kushoto (yaani Jahanamu), nami nitasema, Watu wangu, watu wangu." Hapo itasemwa, "Wewe hujui mambo mapya waliyoyaleta baada yako." Nami nitasema kama alivyosema mtu mwema, Isa, "Nilikuwa shahidi wao nilipokuwa pamoja nao, lakini Uliponifisha Wewe Ukawa Mchungaji wao" (Bukhari, sura *Tafsir)*.

Kufa kwa Nabii Isa kulikotajwa katika Aya hiyo kunahakikishwa na maneno ya Mtume *s.a.w.* ambayo tumeyanakili hapa juu. Sehemu hii inaonyesha kuwa (1) Nabii Isa amekufa si hai kama wanavyodhani baadhi ya Waislamu. (2) Kifo chake ndicho kilifanya atengane na watu wake. (3) Watu wake walimwabudu yeye na mama yake baada ya kufa kwake; alipokuwa nao hawakupotea. (4) Hatarudi yeye mwenyewe, maana angekuwa wa kurudi angewaona Wakristo wanavyopotea, na asingekwenda sema mbele ya Allah kuwa hana habari ya kupotea kwa Wakristo na hali alisha waona. (Soma habari zaidi katika sura 3:56 na 4:159).

اِنۡ تُعَذِّبۡهُمۡ فَاِنَّهُمۡ عِبَادُكَ ۚ وَ اِنۡ تَغۡفِرۡ لَهُمۡ فَاِنَّكَ اَنۡتَ الۡعَزِيۡزُ الۡحَكِيۡمُ ﴿۱۱۹﴾

119. Ikiwa Utawaadhibu, basi bila shaka hao ni watu Wako; na kama Ukiwasamehe basi kwa hakika Wewe ndiwe Mwenye nguvu, Mwenye hekima.

قَالَ اللّٰهُ هٰذَا يَوۡمُ يَنۡفَعُ الصّٰدِقِيۡنَ صِدۡقُهُمۡ ؕ لَهُمۡ جَنّٰتٌ تَجۡرِىۡ مِنۡ تَحۡتِهَا الۡاَنۡهٰرُ خٰلِدِيۡنَ فِيۡهَاۤ اَبَدًا ؕ رَضِىَ اللّٰهُ عَنۡهُمۡ وَرَضُوۡا عَنۡهُ ؕ ذٰلِكَ الۡفَوۡزُ الۡعَظِيۡمُ ﴿۱۲۰﴾

120. Allah Atasema: Hii ndio Siku wasemao kweli utawafaa ukweli wao, wao watazipata bustani zipitazo mito ndani yao, humo watakaa milele. Allah Amewawia radhi, nao wamekuwa radhi naye; huu ndio ufaulu mkuu.

لِلّٰهِ مُلۡكُ السَّمٰوٰتِ وَالۡاَرۡضِ وَمَا فِيۡهِنَّ ؕ وَهُوَ عَلٰى كُلِّ شَىۡءٍ قَدِيۡرٌ ﴿۱۲۱﴾ ع

121. Allah ndiye Mwenye ufalme wa mbingu na ardhi na vilivyomo; Naye ni Mweza juu ya kila kitu.

سُوْرَةُ الْاَنْعَامِ مَكِّيَّةٌ وَّ هِيَ مَعَ الْبَسْمَلَةِ مِائَةٌ وَّ سِتٌّ وَّ سِتُّوْنَ اٰيَةً وَّ عِشْرُوْنَ رُكُوْعًا

6. SURA AL-AN'AAM

Imeteremshwa Makka

Ina mafungu 20 na Aya 166 pamoja na Bismillahi

بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ ①

1. Kwa jina la Allah, Mwingi wa rehema, Mwingi wa ukarimu.

اَلْحَمْدُ لِلّٰهِ الَّذِيْ خَلَقَ السَّمٰوٰتِ وَالْاَرْضَ وَجَعَلَ الظُّلُمٰتِ وَالنُّوْرَ ؕ ثُمَّ الَّذِيْنَ كَفَرُوْا بِرَبِّهِمْ يَعْدِلُوْنَ ②

2. Sifa zote njema zinamhusu Allah Aliyeumba mbingu na ardhi, na Akafanya giza na nuru; juu ya hayo wale waliokufuru wanamwekea Mola wao washirika.

هُوَ الَّذِيْ خَلَقَكُمْ مِّنْ طِيْنٍ ثُمَّ قَضٰٓى اَجَلًا ؕ وَ اَجَلٌ مُّسَمًّى عِنْدَهٗ ثُمَّ اَنْتُمْ تَمْتَرُوْنَ ③

3. Yeye ndiye Amewaumbeni kwa udongo kisha Akaweka muda, na muda maalumu uko Kwake. Juu ya hayo mnafanya shaka.

وَهُوَ اللّٰهُ فِي السَّمٰوٰتِ وَفِي الْاَرْضِ ؕ يَعْلَمُ سِرَّكُمْ وَجَهْرَكُمْ وَيَعْلَمُ مَا تَكْسِبُوْنَ ④

4. Na Yeye ndiye Allah katika mbingu na katika ardhi; Anajua siri zenu na dhahiri zenu. Na Anayajua mnayoyachuma.

وَمَا تَاْتِيْهِمْ مِّنْ اٰيَةٍ مِّنْ اٰيٰتِ رَبِّهِمْ اِلَّا كَانُوْا عَنْهَا مُعْرِضِيْنَ ⑤

5. Na haiwafikii Ishara yo yote katika Ishara za Mola wao ila wanaikengeuka.

فَقَدْ كَذَّبُوْا بِالْحَقِّ لَمَّا جَآءَهُمْ ؕ فَسَوْفَ يَاْتِيْهِمْ اَنْۢبٰٓؤُا مَا كَانُوْا بِهٖ يَسْتَهْزِءُوْنَ ⑥

6. Na wameikadhibisha haki ilipowafikia, kwa hiyo zitawafikia tu habari za yale waliyokuwa wakiyafanyia mzaha.

اَلَمْ يَرَوْا كَمْ اَهْلَكْنَا مِنْ قَبْلِهِمْ مِّنْ قَرْنٍ مَّكَّنّٰهُمْ فِي الْاَرْضِ مَا لَمْ نُمَكِّنْ لَّكُمْ وَاَرْسَلْنَا السَّمَآءَ عَلَيْهِمْ مِّدْرَارًا ۪

7. Je, hawaoni ni vizazi vingapi tulivyoviangamiza kabla yao? Tuliviimarisha katika ardhi Tusivyowaimarisheni ninyi, na Tukayapeleka mawingu juu yao, yakimimina mvua nyingi, na

---

Sura hii ni ya Makka. Taarifa nyingi zaidi zinaeleza ya kuwa yote ilishuka katika sehemu moja; na kama inavyosimuliwa na baadhi ya Muhadithina, Malaika 70,000 walisimama kulinda ilipokuwa ikiteremshwa, na jambo hili linaonyesha jinsi ilivyo heshima ya sura hii katika sura za

وَّجَعَلْنَا الْاَنْهٰرَ تَجْرِیْ مِنْ تَحْتِهِمْ فَاَهْلَكْنٰهُمْ بِذُنُوْبِهِمْ وَاَنْشَاْنَا مِنْۢ بَعْدِهِمْ قَرْنًا اٰخَرِیْنَ ۝٦

Tukaifanya mito ipite chini yao; kisha ndipo Tukawaangamiza kwa sababu ya dhambi zao na Tukaumba baada yao vizazi vingine.

وَلَوْ نَزَّلْنَا عَلَیْكَ كِتٰبًا فِیْ قِرْطَاسٍ فَلَمَسُوْهُ بِاَیْدِیْهِمْ لَقَالَ الَّذِیْنَ كَفَرُوْۤا اِنْ هٰذَاۤ اِلَّا سِحْرٌ مُّبِیْنٌ ۝٧

8. Na lau Tungalikuteremshia mwandiko katika karatasi na wakaugusa kwa mikono yao, bila shaka wale waliokufuru wangalisema: Hii si cho chote ila ni uchawi dhahiri.

وَقَالُوْا لَوْلَاۤ اُنْزِلَ عَلَیْهِ مَلَكٌ ؕ وَلَوْ اَنْزَلْنَا مَلَكًا لَّقُضِیَ الْاَمْرُ ثُمَّ لَا یُنْظَرُوْنَ ۝٨

9. Na husema: Mbona hakuteremshiwa Malaika? Na kama Tungaliteremsha Malaika bila shaka shauri lingalikatwa, kisha wasingalipewa nafasi.

وَلَوْ جَعَلْنٰهُ مَلَكًا لَّجَعَلْنٰهُ رَجُلًا وَّلَلَبَسْنَا عَلَیْهِمْ مَّا یَلْبِسُوْنَ ۝٩

10. Na kama Tungalimfanya Malaika bila shaka Tungalimfanya (kwa sura ya) mtu na Tungaliwatatanishia yale wanayoyatatanisha.

وَلَقَدِ اسْتُهْزِئَ بِرُسُلٍ مِّنْ قَبْلِكَ فَحَاقَ بِالَّذِیْنَ سَخِرُوْا مِنْهُمْ مَّا كَانُوْا بِهٖ یَسْتَهْزِءُوْنَ ۝١٠

11. Na hakika wamefanyiwa mzaha Mitume wa kabla yako, yakawazinga wale waliofanya mzaha miongoni mwao yale waliyokuwa wakiyafanyia mzaha.

FUNGU 2

قُلْ سِیْرُوْا فِی الْاَرْضِ ثُمَّ انْظُرُوْا كَیْفَ كَانَ عَاقِبَةُ الْمُكَذِّبِیْنَ ۝١١

12. Sema: Safirini katika nchi, kisha mtazame ulikuwaje mwisho wa wakadhibishaji.

قُلْ لِّمَنْ مَّا فِی السَّمٰوٰتِ وَالْاَرْضِ ؕ قُلْ لِّلّٰهِ ؕ كَتَبَ عَلٰی نَفْسِهِ الرَّحْمَةَ ؕ لَیَجْمَعَنَّكُمْ اِلٰی یَوْمِ الْقِیٰمَةِ لَا رَیْبَ فِیْهِ ؕ اَلَّذِیْنَ خَسِرُوْۤا اَنْفُسَهُمْ فَهُمْ لَا یُؤْمِنُوْنَ ۝١٢

13. Sema: Ni vya nani vilivyomo mbinguni na ardhini? Sema: Ni vya Allah. Yeye Amejilazimisha kufanya rehema; hakika atawakusanyeni siku ya Kiyama isiyo na shaka ndani yake. Wale waliojitia hasarani basi hao hawataamini.

Qur'an. Imepata jina lake yumkini katika habari iliyoelezwa katika Aya 137-139 ya kuwa wanyama wamekuwa ni katika sababu za kuendeshwa ibada ya masanamu. Mahali pengine (sura 25:45). Qur'an inasema ya kuwa kuabudu masanamu kunawafanya wanaoyaabudu wawe kama wanyama.

Aya 8. Aya hii inaonyesha ya kwamba mtu anapojitupa ndani ya kushukushuku, hakuna jambo lo lote hata liwe wazi linaloweza kumtuliza

وَلَهٗ مَا سَكَنَ فِي الَّيْلِ وَالنَّهَارِ ؕ وَهُوَ السَّمِيْعُ الْعَلِيْمُ ﴿١٤﴾

14. Na ni vyake vinavyokaa katika usiku na mchana; naye ndiye Asikiaye Ajuaye.

قُلْ اَغَيْرَ اللّٰهِ اَتَّخِذُ وَلِيًّا فَاطِرِ السَّمٰوٰتِ وَالْاَرْضِ وَهُوَ يُطْعِمُ وَلَا يُطْعَمُ ؕ قُلْ اِنِّيْٓ اُمِرْتُ اَنْ اَكُوْنَ اَوَّلَ مَنْ اَسْلَمَ وَلَا تَكُوْنَنَّ مِنَ الْمُشْرِكِيْنَ ﴿١٥﴾

15. Sema: Je, nishike mlinzi ghairi ya Allah, Mwumba wa mbingu na ardhi, naye Hulisha wala Halishwi? Sema: Hakika mimi nimeamrishwa niwe wa kwanza wa wenye kusilimu. Nawe usiwe miongoni mwa wanaomshirikisha.

قُلْ اِنِّيْٓ اَخَافُ اِنْ عَصَيْتُ رَبِّيْ عَذَابَ يَوْمٍ عَظِيْمٍ ﴿١٦﴾

16. Sema: Hakika mimi naogopa adhabu ya Siku kubwa ikiwa nitamuasi Mola wangu.

مَنْ يُّصْرَفْ عَنْهُ يَوْمَئِذٍ فَقَدْ رَحِمَهٗ ؕ وَذٰلِكَ الْفَوْزُ الْمُبِيْنُ ﴿١٧﴾

17. Atakayeepushwa nayo Siku hiyo bila shaka amemrehemu; na huo ndio ufaulu dhahiri.

وَاِنْ يَّمْسَسْكَ اللّٰهُ بِضُرٍّ فَلَا كَاشِفَ لَهٗٓ اِلَّا هُوَ ؕ وَاِنْ يَّمْسَسْكَ بِخَيْرٍ فَهُوَ عَلٰى كُلِّ شَيْءٍ قَدِيْرٌ ﴿١٨﴾

18. Na kama Allah Akikugusisha taabu, basi hakuna ye yote awezaye kuiondoa ila Yeye; na kama Akikugusisha heri basi Yeye ni Mwenye uwezo wa kufanya yale yote Atakayo.

وَهُوَ الْقَاهِرُ فَوْقَ عِبَادِهٖ ؕ وَهُوَ الْحَكِيْمُ الْخَبِيْرُ ﴿١٩﴾

19. Na Yeye ni Mwenye uwezo wote juu ya viumbe Vyake na ni Mwenye hekima, Mwenye habari.

قُلْ اَيُّ شَيْءٍ اَكْبَرُ شَهَادَةً ؕ قُلِ اللّٰهُ ۙ شَهِيْدٌۢ بَيْنِيْ وَبَيْنَكُمْ ۫ وَاُوْحِيَ اِلَيَّ هٰذَا الْقُرْاٰنُ لِاُنْذِرَكُمْ بِهٖ وَمَنْۢ بَلَغَ ؕ اَئِنَّكُمْ لَتَشْهَدُوْنَ اَنَّ مَعَ اللّٰهِ اٰلِهَةً

20. Sema: Kitu gani ni kikubwa zaidi kwa kutoa ushahidi? Sema: Allah ndiye Shahidi baina yangu na baina yenu; na Qur'an hii imefunuliwa kwangu ili kwayo niwaonyeni ninyi na yule imfikiayo. Je, kwa yakini ninyi mnashuhudia ya kwamba wako miungu wengine pamoja na Allah? Sema: Mimi

---

Aya 15. *Nimeamrishwa niwe wa kwanza wa wenye kusilimu.* Padre Dale anaifasiri Aya hii hivi, "Yaani, Mwarabu wa kwanza. Basi Ibrahimu na Ishmael walipoijenga Kaaba, hapakuwa na Waarabu walioshika imani ya Ibrahimu hanifi?" (uk. 587, 588 wa Tafsiri yake).

sishuhudii. Sema, Yeye ni Mungu Mmoja tu, na mimi ni mbali na hayo mnayoyashirikisha.

21. Wale Tuliowapa Kitabu, humfahamu kama wanavyowafahamu wana wao. Wale waliojitia hasarani, wao hawataamini.

اُخْرٰى ؕ قُلْ لَّاۤ اَشْهَدُ ۚ قُلْ اِنَّمَا هُوَ اِلٰهٌ
وَّاحِدٌ وَّاِنَّنِيْ بَرِيْٓءٌ مِّمَّا تُشْرِكُوْنَ ۝٢٠ وقف لازم
اَلَّذِيْنَ اٰتَيْنٰهُمُ الْكِتٰبَ يَعْرِفُوْنَهٗ كَمَا
يَعْرِفُوْنَ اَبْنَآءَهُمْ ؕ اَلَّذِيْنَ خَسِرُوْٓا وقف لازم
اَنْفُسَهُمْ فَهُمْ لَا يُؤْمِنُوْنَ ۝٢١ ع ٢ ٨

Swali hili halionyeshi kama Padre Dale alikuwa mtu mwenye fikira za kialimu. Aya hii ni wazi sana. Mtume Muhammad *s.a.w.* ndiye aliyeileta dini ya Kiislamu kwa watu waliokuwa hawaijui.
Ni dhahiri yeye mwenyewe ni mtu wa kwanza miongoni mwao aliyeshika Uislamu. Hivyo suali hili la Padre Dale linaonyesha kuhangaika ovyo. watu husema uadui ni upofu. Dini ya Kiislamu inakiri ya kuwa Manabii wote waliotangulia pamoja na wafuasi wao walikuwa "Muslimiin" yaani watu waliojitupa kwa Allah.

PADRE DALE AMEPENYEZA NENO.

Maneno haya, "Niwe wa kwanza katika wenye kusilimu" siyo maana yake "Mwarabu wa kwanza" kama unavyotaka upekepeke wa Padre Dale. Dini ya Kiislamu haikuja kwa ajili ya Waarabu peke yao, bali kwa ajili ya watu wote. Allah asingeshindwa kumwambia Mtume aseme kuwa ameamrishwa "kuwa Mwarabu wa kwanza." Lakini neno *Mwarabu* hakuna katika Aya, na tunaghairi sana upekepeke huu wa Padre Dale wa kujitia katika mambo asiyoyajua, maneno haya "niwe wa kwanza" maana yake ni kama yalivyo. Unaweza kuyafasiri "Niwe (mtu) wa kwanza" kwa kuwa Mtume *s.a.w.* alikuwa mtu wa kwanza katika umati wake wenye makabila ya Waarabu, Waafrika, Wahindi, Wazungu, Wachina na k.w.k; na kwa watu wote aliotumwa kwao, yeye ni wa kwanza kusilimu.

NABII MUSA ALISEMA MANENO HAYO.

Nabii Musa pia alisema maneno ya namna hiyo, "Na mimi ni wa kwanza wa waaminio" (sura 7:144). Je, itakuwa ni uaminifu kufumba macho na kufasiri maneno hayo kuwa Musa ndiye alikuwa Mwisraeli wa kwanza kuamini, na kabla yake hakukuwa mtoto mwingine wa Yakubu aliyeamini? Maneno haya hayaonyeshi ila ya kwamba, katika umati wake Musa mwenyewe ndiye alikuwa wa kwanza kuamini.

WACHAWI PIA WALISEMA HAYO.

Wachawi wa Firauni pia, waliposhindwa na Musa, walisema: "Tunatumai ya kwamba Mola wetu Atatusamehe makosa yetu, maana sisi tumekuwa wa kwanza wa waaminio" (sura 16:52). Padre Dale, tunamwona mara kwa mara, kwanza analeta tafsiri ya makosa, kisha anawahoji Waislamu juu ya msingi wa kosa lake mwenyewe. Au, anaacha Qur'an inavyosema, anashika masimulizi asiyoweza kuyatolea ushahidi, kisha anaanza kuishambulia Qur'an juu ya msingi wa masimulizi hayo. Watu husema njia ya mwongo ni fupi. Padre Dale hakudhani kuwa Allah Ataleta watu watakaodhihirisha udanganyifu wa kitabu chake. Mungu Aliahidi kuilinda Qur'an Yake, basi jihadharini na kuiparamia!

Aya 21. *Humfahamu kama wanavyowafahamu wana wao.* Mtume au jambo la imani huwa halijulikani mwanzoni kama mtu anavyolitambua jua au mwezi. Mtume hutambuliwa kama baba anavyomtambua mwanawe, anajua inayumkinika kabisa kuwa mtoto ni wake ingawa hawezi kusema kuwa ana yakini.

FUNGU 3

وَمَنْ اَظْلَمُ مِمَّنِ افْتَرٰى عَلَى اللّٰهِ كَذِبًا اَوْ كَذَّبَ بِاٰيٰتِهٖ ؕ اِنَّهٗ لَا يُفْلِحُ الظّٰلِمُوْنَ ﴿۲۱﴾

22. Na nani mdhalimu mkubwa kuliko yule amtungiaye uwongo Allah au azikadhibishaye Ishara Zake? Hakika wadhalimu hawatafaulu.

وَيَوْمَ نَحْشُرُهُمْ جَمِيْعًا ثُمَّ نَقُوْلُ لِلَّذِيْنَ اَشْرَكُوْٓا اَيْنَ شُرَكَآؤُكُمُ الَّذِيْنَ كُنْتُمْ تَزْعُمُوْنَ ﴿۲۲﴾

23. Na siku ambayo Tutawakusanya wote pamoja, kisha Tutawaambia wale walioshirikisha: Wako wapi washirika wenu mliokuwa mnadai?

ثُمَّ لَمْ تَكُنْ فِتْنَتُهُمْ اِلَّآ اَنْ قَالُوْا وَاللّٰهِ رَبِّنَا مَا كُنَّا مُشْرِكِيْنَ ﴿۲۳﴾

24. Kisha hautakuwa udhuru wao isipokuwa kusema: Wallahi, Mola wetu hatukuwa washirikina.

اُنْظُرْ كَيْفَ كَذَبُوْا عَلٰٓى اَنْفُسِهِمْ وَضَلَّ عَنْهُمْ مَّا كَانُوْا يَفْتَرُوْنَ ﴿۲۴﴾

25. Angalia jinsi wasemavyo uwongo dhidi yao wenyewe. Na yamewapotea waliyokuwa wakiyatunga.

وَمِنْهُمْ مَّنْ يَّسْتَمِعُ اِلَيْكَ ۚ وَجَعَلْنَا عَلٰى قُلُوْبِهِمْ اَكِنَّةً اَنْ يَّفْقَهُوْهُ وَفِيْٓ اٰذَانِهِمْ وَقْرًا ؕ وَاِنْ يَّرَوْا كُلَّ اٰيَةٍ لَّا يُؤْمِنُوْا بِهَا ؕ حَتّٰٓى اِذَا جَآءُوْكَ يُجَادِلُوْنَكَ يَقُوْلُ الَّذِيْنَ كَفَرُوْٓا اِنْ هٰذَآ اِلَّآ اَسَاطِيْرُ الْاَوَّلِيْنَ ﴿۲۵﴾

26. Na yuko miongoni mwao anayekusikiliza, na Tumetia pazia mioyoni mwao wasije kuyafahamu, na mna uzito masikioni mwao; na ijapokuwa waone kila Ishara hawataia-mini; hata wanapokufikia wanakujadili; wale waliokufuru wanasema: Hizi si cho chote ila ni hadithi tu za watu wa kale.

وَهُمْ يَنْهَوْنَ عَنْهُ وَيَنْـَٔوْنَ عَنْهُ ۚ وَاِنْ يُّهْلِكُوْنَ اِلَّآ اَنْفُسَهُمْ وَمَا يَشْعُرُوْنَ ﴿۲۶﴾

27. Nao wanakataza hayo na wenyewe wanajiweka mbali nayo; nao hawaangamizi ila nafsi zao hali hawatambui.

Aya 22. Hapa ni wazi ya kuwa maadamu Allah Anamsaidia Mtume Muhammad *s.a.w.*, na anamfanya afanikiwe mbele ya uadui na upinzani, ni alama ya wazi itokayo kwa Mungu ya kuwa yeye ni Mtume wa kweli

Aya 26. *Ni hadithi za watu wa kale*. Qur'an inasema, habari inazozisimulia ni "Ishara," lakini wasioamini wanaziita "hadithi za watu wa kale" na Allah analaumu huo usemi wao. Jambo hili linaonyesha ya kuwa mbele ya Allah habari za Manabii na watu waliopita zamani zilizomo ndani ya Qur'an hazikusudiwi kuwa "masimulizi" au "hadithi," bali ni "Ishara" zinazotabiri matokeo ya baadaye ambayo yanapotimia yanakuwa "Ishara."

وَلَوْ تَرٰٓى اِذْ وُقِفُوْا عَلَى النَّارِ فَقَالُوْا يٰلَيْتَنَا نُرَدُّ وَلَا نُكَذِّبَ بِاٰيٰتِ رَبِّنَا وَنَكُوْنَ مِنَ الْمُؤْمِنِيْنَ ﴿٢٨﴾

28. Na ungeona watakaposimamishwa juu ya Moto, ndipo watasema; Laiti tungerudishwa na kutozikadhibisha Aya za Mola wetu na kuwa miongoni mwa waaminio.

بَلْ بَدَا لَهُمْ مَّا كَانُوْا يُخْفُوْنَ مِنْ قَبْلُ ؕ وَلَوْ رُدُّوْا لَعَادُوْا لِمَا نُهُوْا عَنْهُ وَاِنَّهُمْ لَكٰذِبُوْنَ ﴿٢٩﴾

29. Siyo! Yatawadhihirikia waliyokuwa wakiyaficha zamani. Na kama wangalirudishwa bila shaka wangeyarudia yale waliyokatazwa, na bila shaka hao ni waongo tu.

وَقَالُوْٓا اِنْ هِيَ اِلَّا حَيَاتُنَا الدُّنْيَا وَمَا نَحْنُ بِمَبْعُوْثِيْنَ ﴿٣٠﴾

30. Na husema: Haya sio ila ni maisha yetu ya dunia tu, wala sisi hatutafufuliwa.

وَلَوْ تَرٰٓى اِذْ وُقِفُوْا عَلٰى رَبِّهِمْ ؕ قَالَ اَلَيْسَ هٰذَا بِالْحَقِّ ؕ قَالُوْا بَلٰى وَرَبِّنَا ؕ قَالَ فَذُوْقُوا الْعَذَابَ بِمَا كُنْتُمْ تَكْفُرُوْنَ ﴿٣١﴾ ع

31. Na ungewaona watakaposimamishwa mbele ya Mola wao, Yeye Atasema: Je, hiyo si haki? Watasema: Naam, kwa haki ya Mola wetu. Atasema: Basi ionjeni adhabu kwa sababu mlikuwa mkikataa.

FUNGU 4

قَدْ خَسِرَ الَّذِيْنَ كَذَّبُوْا بِلِقَآءِ اللّٰهِ ؕ حَتّٰٓى اِذَا جَآءَتْهُمُ السَّاعَةُ بَغْتَةً قَالُوْا يٰحَسْرَتَنَا عَلٰى مَا فَرَّطْنَا فِيْهَا ۙ وَهُمْ يَحْمِلُوْنَ اَوْزَارَهُمْ عَلٰى ظُهُوْرِهِمْ ؕ اَلَا سَآءَ مَا يَزِرُوْنَ ﴿٣٢﴾

32. Bila shaka wamekwisha pata hasara wale waliokadhibisha kukutana na Allah; hata itakapowafikia saa ile kwa ghafla, watasema: Oo! Majuto yetu juu ya yale tuliyopuuza! Nao watabeba mizigo (ya madhambi) yao migongoni mwao. Angalieni ni mabaya wanayoyabeba.

وَمَا الْحَيٰوةُ الدُّنْيَآ اِلَّا لَعِبٌ وَّ لَهْوٌ ؕ وَلَلدَّارُ الْاٰخِرَةُ خَيْرٌ لِّلَّذِيْنَ يَتَّقُوْنَ ؕ اَفَلَا تَعْقِلُوْنَ ﴿٣٣﴾

33. Na maisha ya dunia hii si kitu ila mchezo na upuuzi, na bila shaka nyumba ya Akhera ni bora zaidi kwa wale wamchao (Allah); basi je hamtumii akili?

Aya 30. Watu wengi huzama katika anasa na starehe za dunia hata wasiweze kukaa na kufikiri mauti na Akhera, na kudhani hawatafufuliwa.

Aya 33. Aya hii inafahamisha ya kuwa mambo ya dunia hii, mtu akikaa bila hadhari, yanaweza kumfanya aanze kupuuza habari za Akhera, kama vile michezo mara nyingi humfanya mtu apuuze mambo yaliyo wajibu kwake.

قَدْ نَعْلَمُ اِنَّهٗ لَيَحْزُنُكَ الَّذِىْ يَقُوْلُوْنَ فَاِنَّهُمْ لَا يُكَذِّبُوْنَكَ وَلٰكِنَّ الظّٰلِمِيْنَ بِاٰيٰتِ اللّٰهِ يَجْحَدُوْنَ ﴿٣٤﴾

34. Hakika Tunajua ya kwamba yanakuhuzunisha yale wanayoyasema. Basi hao hawakukadhibishi, lakini wadhalimu wanakanusha Ishara za Allah.

وَلَقَدْ كُذِّبَتْ رُسُلٌ مِّنْ قَبْلِكَ فَصَبَرُوْا عَلٰى مَا كُذِّبُوْا وَاُوْذُوْا حَتّٰٓى اَتٰىهُمْ نَصْرُنَا ۚ وَلَا مُبَدِّلَ لِكَلِمٰتِ اللّٰهِ ۚ وَلَقَدْ جَآءَكَ مِنْ نَّبَاِى الْمُرْسَلِيْنَ ﴿٣٥﴾

35. Na hakika wamekadhibishwa Mitume kabla yako, lakini walivumilia juu ya kukadhibishwa na kuudhiwa, mpaka ukawafikia msaada Wetu. Na hakuna wa kubadilisha maneno ya Allah, na bila shaka zimekufikia baadhi ya habari za Mitume.

وَاِنْ كَانَ كَبُرَ عَلَيْكَ اِعْرَاضُهُمْ فَاِنِ اسْتَطَعْتَ اَنْ تَبْتَغِىَ نَفَقًا فِى الْاَرْضِ اَوْ سُلَّمًا فِى السَّمَآءِ فَتَاْتِيَهُمْ بِاٰيَةٍ ۭ وَلَوْ شَآءَ اللّٰهُ لَجَمَعَهُمْ عَلَى الْهُدٰى فَلَا تَكُوْنَنَّ مِنَ الْجٰهِلِيْنَ ﴿٣٦﴾

36. Na ikiwa kujitenga kwao ni chukizo kwako, basi kama unaweza kutafuta tundu katika ardhi au ngazi mbinguni na kuwaletea Ishara (fanya hivyo). Na kama Allah Angependa bila shaka Angaliwakusanya kwenye mwongozo, hivyo usiwe miongoni mwa wajinga.

Aya 35. *Hakuna abadilishaye maneno ya Allah.* (1) Maneno ya mwanzo wa Aya hii yanaonyesha ya kuwa Allah anamwambia Mtume maneno ya kumfariji ya kuwa, Tunajua unapata taabu na unasumbuliwa, na Mitume wa zamanni pia walipata taabu namna hiyo mwanzoni, na mwishoni msaada Wetu ukawafikia, nao wakafanikiwa. Basi hayo ndio maneno ya Allah toka zamani juu ya Mitume wake ya kwamba, ingawa wao ndio watashinda, lakini watateswa na kusumbuliwa, na Allah hawalazimishi hao maadui zao kukubali haki. Hayo ndio maneno ya Allah, nayo hayabadilishwi.

(2) Kama Allah ametoa ahadi, hakuna awezaye kuibadilisha ahadi hiyo; lazima itatimia. Kwa mfano Allah aliahidi kuilinda Qur'an (sura 15:10), nayo imelindwa salama kabisa hata hakuna nukta moja iliyopotea, nayo ni ile ile leo, kama ilivyokuwa siku za Mtume mwenyewe; hakuna aliyeweza kuzidisha au kupunguza neno lo lote ndani yake. Lakini Vitabu vya Manabii wa zamani Allah hakuahidi kuvilinda kwa kuwa havikukusudiwa kudumu milele. Basi viliharibika na vinaendelea kuharibika. Watu wanapenyeza ndani ya Vitabu hivyo maneno yasiyokuwemo na wakiondoa mengine wasiyoyataka. Kwa mfano Vitabu vya Biblia Mungu hakuahidi kuvilinda, hivyo vimeharibika kabisa leo. Soma maelezo ya sura 2:43 na 5:14.

Aya 36. *Nafaq.* "Tundu" maana yake ni tundu au njia iliyotobolewa katika ardhi na iko wazi upande wa pili (Akrab).

Maneno haya, *kutafuta tundu katika ardhi,* yanaonyesha kutumia njia za kidunia, yaani kuhubiri na kueneza ukweli duniani ili kuipa dini nguvu; na maneno *ngazi mbinguni,* yanaonyesha kutumia njia za kiroho; yaani kuwaombea kwa Allah wasioamini waongozwe n.k.w. Kwa hakika maombi ni ngazi inayomwezesha mtu kupanda mbinguni. Hapa Mtume *s.a.w.*

37. Wanaoitikia ni wale tu wanaosikiliza. Na ama wafu Allah Atawafufua, kisha watarejeshwa Kwake.

إِنَّمَا يَسْتَجِيبُ الَّذِينَ يَسْمَعُونَ ۘ وَالْمَوْتَىٰ يَبْعَثُهُمُ اللَّهُ ثُمَّ إِلَيْهِ يُرْجَعُونَ ﴿٣٧﴾

anaambiwa kuwa Allah hatawashurutisha watu kukubali Uislamu. Kama anataka watu waingie dini kwa wingi, basi afuate hizo njia mbili alizoonyeshwa.

UBISHI WA PADRE DALE.

Padre Dale anasema' "Muhammad mara nyingi alisema ya kuwa hakupewa miujiza. Basi mbona Waislamu wa siku hizi wanasema ya kuwa alipewa miujiza mingi tangu utoto wake mpaka kufa kwake?" (uk. 588 wa Tafsiri yake). Maneno yanaonyesha Padre Dale ameshindwa kufahamu Aya hii. Maelezo tuliyoandika hapo hayaonyeshi kuwa Aya hii inakataa kuonyesha miujiza. Aya hii inaonyesha ya kuwa Mwenyezi Mungu hatawashurutisha watu kukubali dini kwa nguvu. Lakini Ishara ya kufunua akili zao ili waone haki itafika kama Mtume s.a.w. akikazana kuhubiri na kuomba kwa Allah.

Hata tafsiri aliyoandika Padre mwenyewe juu ya Aya hii haionyeshi kukataa kuonyesha Ishara. Yeye ameifasiri hivi Aya hiyo. "Na ikiwa kujitenga kwao nawe ni neno kubwa kwako, basi ukiweza kutafuta shimo la kuingilia ardhini, au ngazi ya kupanda mbinguni ili kuwaletea ishara *fanya hivi*; na kama Mungu angependa, hakika angewaleta wote pia kwenye mwongozo." (uk. 120).

QUR'AN INAAHIDI KUONYESHA ISHARA.

Je, tafsiri hiyo inakataa wapi kuonyesha Ishara? Maneno hayo yanaonyesha tu kuwa Mungu hapendi kuwashurutisha watu kuingia dini, lakini kama Mtume atafute tundu la ardhi, yaani, njia za kidunia za kueneza dini, na ngazi ya kupandia mbinguni, yaani, kuomba sana kwa Allah, basi bila shaka Ishara za kuwafanya makafiri waingie dini zitatokea. Na ndivyo ilivyokuwa, haukupita muda mrefu ila Waarabu wote waliingia Uislamu Mtume mwenyewe angali hai. Ingekuwa vizuri wakatuambia Ishara alizofanya Yesu zilileta matokeo gani katika maisha yake.

Katika sura 57:10 tunasoma. "Yeye ndiye anayeteremsha Ishara zilizo wazi juu ya Mtumishi Wake ili kuwatoeni katika giza mwende kwenye nuru." Je, tuseme Padre Dale hakuona Aya kama hii zinazoonyesha wazi kuwa miujiza ilikuwa ikionyeshwa? La, Padre Dale anajua Aya za namna hii ziko. Katika tafsiri yake ameitafsiri hivi Aya hiyo: "Yeye ndiye aliyemteremshia mtumishi wake ishara wazi apate kuwatoeni katika giza na kuwaleta kwenye nuru" (uk. 485). Ingawa neno la Kiarabu (*Yunazzilu* maana yake ni *Atateremsha, Anateremsha* au *Huteremsha* yeye kalifasiri *Aliteremsha*; hata hivyo ni wazi kuwa miujiza na ishara vilitokea). Sasa inampasaje Padre Dale Canon mzima wa kanisa la Yesu la Unguja, kuzua uwongo kwamba "Muhammad mara nyingi alisema ya kwamba hakupewa miujiza?" Yesu ndiye alisema hataonyesha miujiza. Imeandikwa, "Wakatokea mafarisayo, wakaanza kuhojiana naye; wakitafuta kwake Ishara itokayo mbinguni: wakimjaribu. Akaugua rohoni mwake akasema. Mbona kizazi hiki chatafuta Ishara? Amin, nawaambieni, Hakitapewa Ishara kizazi hiki" (Marko 8:11-12). Nasi tunawauliza Wakristo swali lile lile alilotuuliza Padre, "Basi mbona Wakristo wa siku hizi wanasema ya kuwa Yesu alifanya miujiza mingi na hali Yesu mwenyewe alisema kizazi kile hakitapewa ishara?" Habari za miujiza ya Yesu soma maelezo ya sura 3:60.

Aya 37. Aya inaonyesha ya kuwa watu wenye mioyo mizuri na wanaokubali kusikiliza watakuwa tayari kukubali haki. Na ama wale walio wafu wa roho na ambao wanaweza kuongozwa,

وَقَالُوْا لَوْلَا نُزِّلَ عَلَيْهِ اٰيَةٌ مِّنْ رَّبِّهٖ ؕ قُلْ اِنَّ اللّٰهَ قَادِرٌ عَلٰٓى اَنْ يُّنَزِّلَ اٰيَةً وَّلٰكِنَّ اَكْثَرَهُمْ لَا يَعْلَمُوْنَ ﴿٣٨﴾

38. Na husema: Mbona hakuteremshiwa Ishara kutoka kwa Mola wake? Sema: Hakika Allah ni Mwenye uwezo wa kuteremsha Ishara, lakini wengi wao hawajui.

وَمَا مِنْ دَآبَّةٍ فِى الْاَرْضِ وَلَا طٰٓئِرٍ يَّطِيْرُ بِجَنَاحَيْهِ اِلَّآ اُمَمٌ اَمْثَالُكُمْ ؕ مَا فَرَّطْنَا فِى الْكِتٰبِ مِنْ شَىْءٍ ثُمَّ اِلٰى رَبِّهِمْ يُحْشَرُوْنَ ﴿٣٩﴾

39. Na hakuna mnyama katika ardhi wala ndege arukae kwa mbawa zake mbili, ila ni nyimati kama ninyi. Hatukupuuza Kitabuni kitu chochote. Kisha watakusanywa kwa Mola wao.

وَالَّذِيْنَ كَذَّبُوْا بِاٰيٰتِنَا صُمٌّ وَّبُكْمٌ فِى الظُّلُمٰتِ ؕ مَنْ يَّشَاِ اللّٰهُ يُضْلِلْهُ ؕ وَمَنْ يَّشَاْ يَجْعَلْهُ عَلٰى صِرَاطٍ مُّسْتَقِيْمٍ ﴿٤٠﴾

40. Na wale waliozikadhibisha Ishara Zetu ni viziwi na mabubu waliomo gizani. Amtakaye Allah Humhukumu kupotea, Na Amtakaye Humuweka katika njia iliyonyooka.

قُلْ اَرَءَيْتَكُمْ اِنْ اَتٰىكُمْ عَذَابُ اللّٰهِ اَوْ اَتَتْكُمُ السَّاعَةُ اَغَيْرَ اللّٰهِ تَدْعُوْنَ ۚ اِنْ كُنْتُمْ صٰدِقِيْنَ ﴿٤١﴾

41. Sema: Niambieni! kama ikiwafikieni adhabu ya Allah au iwafikieni saa ile, je mtamwita ye yote asiyekuwa Allah ikiwa ninyi ni wakweli?

بَلْ اِيَّاهُ تَدْعُوْنَ فَيَكْشِفُ مَا تَدْعُوْنَ اِلَيْهِ اِنْ شَآءَ وَتَنْسَوْنَ مَا تُشْرِكُوْنَ ﴿٤٢﴾ ع ١٤

42. Bali Yeye ndiye mtamwita, naye Atawaondoleeni mnayomwitia, Akipenda, na mtayasahau mnayoshirikisha.

FUNGU 5

وَلَقَدْ اَرْسَلْنَآ اِلٰٓى اُمَمٍ مِّنْ قَبْلِكَ فَاَخَذْنٰهُمْ بِالْبَاْسَآءِ وَالضَّرَّآءِ لَعَلَّهُمْ يَتَضَرَّعُوْنَ ﴿٤٣﴾

43. Na kwa yakini Tulipeleka (Mitume) kwa watu waliokuwa kabla yako; kisha Tukawakamata kwa dhiki na madhara ili wapate kunyenyekea.

Mungu atawafufua kwa kuwaonyesha Ishara,kisha nao watasikiliza na kuukubali Uislamu.Hivi ndivyo ilivyotokea, Allah alipoonyesha Ishara Yake wakati iliposhindwa Makka, Bara Arabu nzima iliingia katika dini ya Kiislamu, na neno hilo la Mungu likatimia.

فَلَوْلَآ اِذْ جَآءَهُمْ بَاْسُنَا تَضَرَّعُوْا وَلٰكِنْ قَسَتْ قُلُوْبُهُمْ وَ زَيَّنَ لَهُمُ الشَّيْطٰنُ مَا كَانُوْا يَعْمَلُوْنَ ﴿٤٤﴾

44. Basi mbona hawakunyenyekea ilipowafikia adhabu Yetu? Lakini mioyo yao ikawa migumu, na Shetani akawapambia waliyokuwa wakiyafanya.

فَلَمَّا نَسُوْا مَا ذُكِّرُوْا بِهٖ فَتَحْنَا عَلَيْهِمْ اَبْوَابَ كُلِّ شَيْءٍ ؕ حَتّٰٓى اِذَا فَرِحُوْا بِمَآ اُوْتُوْٓا اَخَذْنٰهُمْ بَغْتَةً فَاِذَا هُمْ مُّبْلِسُوْنَ ﴿٤٥﴾

45. Basi waliposahau yale waliyokumbushwa Tukawafungulia milango ya kila kitu, mpaka walipofurahia yale waliyopewa Tukawashika ghafla; na mara wakawa wenye kukata tamaa.

فَقُطِعَ دَابِرُ الْقَوْمِ الَّذِيْنَ ظَلَمُوْا ؕ وَالْحَمْدُ لِلّٰهِ رَبِّ الْعٰلَمِيْنَ ﴿٤٦﴾

46. Kwa hiyo ikakatwa mizizi ya watu waliodhulumu; na sifa zote njema humhusu Allah. Mola wa walimwengu.

قُلْ اَرَءَيْتُمْ اِنْ اَخَذَ اللّٰهُ سَمْعَكُمْ وَاَبْصَارَكُمْ وَخَتَمَ عَلٰى قُلُوْبِكُمْ مَّنْ اِلٰهٌ غَيْرُ اللّٰهِ يَاْتِيْكُمْ بِهٖ ؕ اُنْظُرْ كَيْفَ نُصَرِّفُ الْاٰيٰتِ ثُمَّ هُمْ يَصْدِفُوْنَ ﴿٤٧﴾

47. Sema: Niambieni, kama Allah Akiwaondoleeni kusikia kwenu na kuona kwenu na kuipiga muhuri mioyo yenu, ni nani mungu mwingine isipokuwa Allah Awezaye kuwaleteeni tena? Tazama jinsi Tunavyoeleza Aya, kisha wao wanapinduka.

قُلْ اَرَءَيْتَكُمْ اِنْ اَتٰىكُمْ عَذَابُ اللّٰهِ بَغْتَةً اَوْ جَهْرَةً هَلْ يُهْلَكُ اِلَّا الْقَوْمُ الظّٰلِمُوْنَ ﴿٤٨﴾

48. Sema: Niambieni kama iwafikieni kwa ghafla adhabu ya Allah au kwa dhahiri, nani wataangamizwa isipokuwa watu waliodhulumu?

وَمَا نُرْسِلُ الْمُرْسَلِيْنَ اِلَّا مُبَشِّرِيْنَ وَمُنْذِرِيْنَ ۚ فَمَنْ اٰمَنَ وَاَصْلَحَ فَلَا خَوْفٌ عَلَيْهِمْ وَلَا هُمْ يَحْزَنُوْنَ ﴿٤٩﴾

49. Na hatutumi Mitume ila watoao habari njema na waonyao. Na wenye kuamini na kufanya wema, basi haitakuwa hofu juu yao, wala hawatahuzunika.

وَالَّذِيْنَ كَذَّبُوْا بِاٰيٰتِنَا يَمَسُّهُمُ الْعَذَابُ بِمَا كَانُوْا يَفْسُقُوْنَ ﴿٥٠﴾

50. Na wale waliozikadhibisha aya Zetu itawagusa adhabu, kwa sababu walikuwa wakiasi.

Aya 46. *Ikakatwa mizizi ya watu waliodhulumu.* "Mizizi" hapa mradi wake ni viongozi wa uasi. Imam Razi anasema, *Daabir* ni mtu wa mwisho aliyebaki kuangalia mambo.

قُلْ لَّآ اَقُوْلُ لَكُمْ عِنْدِيْ خَزَآئِنُ اللّٰهِ وَلَآ اَعْلَمُ الْغَيْبَ وَلَآ اَقُوْلُ لَكُمْ اِنِّيْ مَلَكٌ ۚ اِنْ اَتَّبِعُ اِلَّا مَا يُوْحٰٓى اِلَيَّ ۭ قُلْ هَلْ يَسْتَوِي الْاَعْمٰى وَالْبَصِيْرُ ۭ اَفَلَا تَتَفَكَّرُوْنَ ۝۵۰ ع

51. Sema: Mimi siwaambii, Ninazo hazina za Allah, au najua mambo ya siri; wala siwaambieni, mimi ni Malaika, sifuati ila yaliyofunuliwa kwangu. Sema: Je, kipofu na mwenye kuona wako sawa? Basi je hamtafakari?

FUNGU 6

وَاَنْذِرْ بِهِ الَّذِيْنَ يَخَافُوْنَ اَنْ يُّحْشَرُوْٓا اِلٰى رَبِّهِمْ لَيْسَ لَهُمْ مِّنْ دُوْنِهٖ وَلِيٌّ وَّلَا شَفِيْعٌ لَّعَلَّهُمْ يَتَّقُوْنَ ۝۵۱

52. Na uwaonye kwa (Qur'an) hii wale wanaoogopa ya kwamba watakusanywa kwa Mola wao, hawana mlinzi ye yote isipokuwa Yeye, wala mwombezi, ili wapate kumcha.

وَلَا تَطْرُدِ الَّذِيْنَ يَدْعُوْنَ رَبَّهُمْ بِالْغَدٰوةِ وَالْعَشِيِّ يُرِيْدُوْنَ وَجْهَهٗ ۭ مَا عَلَيْكَ مِنْ حِسَابِهِمْ مِّنْ شَيْءٍ وَّمَا مِنْ حِسَابِكَ عَلَيْهِمْ مِّنْ شَيْءٍ فَتَطْرُدَهُمْ فَتَكُوْنَ مِنَ الظّٰلِمِيْنَ ۝۵۲

53. Wala usiwafukuze wale wanaomuomba Mola wao asubuhi na jioni kwa kutaka radhi Yake; si juu yako hesabu yao hata kidogo wala hesabu yako si juu yao hata kidogo, ya kwamba uwafukuze na uwe miongoni mwa wadhalimu.

وَكَذٰلِكَ فَتَنَّا بَعْضَهُمْ بِبَعْضٍ لِّيَقُوْلُوْٓا اَهٰٓؤُلَاۗءِ مَنَّ اللّٰهُ عَلَيْهِمْ مِّنْۢ بَيْنِنَا ۭ اَلَيْسَ اللّٰهُ بِاَعْلَمَ بِالشّٰكِرِيْنَ ۝۵۳

54. Na kadhalika Tumewajaribu baadhi yao kwa wengine ili waseme: Je, hao ndio Allah Amewafanyia hisani miongoni mwetu? Je, Allah Hawajui sana wanaomshukuru?

وَاِذَا جَاۗءَكَ الَّذِيْنَ يُؤْمِنُوْنَ بِاٰيٰتِنَا فَقُلْ سَلٰمٌ عَلَيْكُمْ كَتَبَ رَبُّكُمْ عَلٰي نَفْسِهِ الرَّحْمَةَ ۙ اَنَّهٗ مَنْ عَمِلَ مِنْكُمْ سُوْۗءًا بِجَهَالَةٍ ثُمَّ تَابَ مِنْۢ بَعْدِهٖ وَاَصْلَحَ فَاَنَّهٗ غَفُوْرٌ رَّحِيْمٌ ۝۵۴

55. Na wanapokufikia wale wanaoamini Aya zetu, basi sema: Amani iwe juu yenu, Mola wenu Amejilazimisha rehema, kwamba atakayefanya miongoni mwenu uovu kwa ujinga, kisha baada yake akatubu na kujirekebisha, basi Yeye Ndiye Msamehevu, Mrehemevu.

وَكَذٰلِكَ نُفَصِّلُ الْاٰيٰتِ وَلِتَسْتَبِيْنَ سَبِيْلُ الْمُجْرِمِيْنَ ۝۵۵ ع

56. Na hivi ndivyo Tunavyoeleza Aya, na ili njia ya wakosefu ibainike.

Aya 53. Siyo mradi wake ya kuwa Mtume *s.a.w.* alikuwa akiwafukuza watu wanyonge walioingia dini. Bali hapa wanajibiwa watu wenye majivuno ambao hukataa kufuata dini kwa kuwa wanaoifuata ni watu wanyonge na maskini, na ambao hutaka wale maskini kwanza wafukuzwe kisha nao ndipo waingie. Hapa watu hao wanaambiwa, hii haja yao haikubaliwi.

FUNGU 7

57. Sema: Hakika nimekatazwa kuwaabudu wale mnaowaita kinyume cha Allah. Sema: Sifuati matamanio yenu, maana hapo nitakuwa nimepotea na sitakuwa miongoni mwa walioongoka.

قُلْ اِنِّیْ نُهِیْتُ اَنْ اَعْبُدَ الَّذِیْنَ تَدْعُوْنَ مِنْ دُوْنِ اللّٰهِ ؕ قُلْ لَّاۤ اَتَّبِعُ اَهْوَآءَكُمْ ۙ قَدْ ضَلَلْتُ اِذًا وَّ مَاۤ اَنَا مِنَ الْمُهْتَدِیْنَ ﴿۵۷﴾

58. Sema: Hakika mimi ninayo dalili wazi itokayo kwa Mola wangu, nanyi mmeikadhibisha; sina mnayoyataka kwa haraka; hukumu ni ya Allah tu, Anahadithia yaliyo kweli; Naye ni Mbora wa mahakimu.

قُلْ اِنِّیْ عَلٰی بَیِّنَةٍ مِّنْ رَّبِّیْ وَ كَذَّبْتُمْ بِهٖ ؕ مَا عِنْدِیْ مَا تَسْتَعْجِلُوْنَ بِهٖ ؕ اِنِ الْحُكْمُ اِلَّا لِلّٰهِ ؕ یَقُصُّ الْحَقَّ وَ هُوَ خَیْرُ الْفٰصِلِیْنَ ﴿۵۸﴾

59. Sema: Lau ningalikuwa nayo mnayoyataka upesi, shauri lingalikatwa baina yangu na baina yenu; na Allah Anawajua sana wadhalimu.

قُلْ لَّوْ اَنَّ عِنْدِیْ مَا تَسْتَعْجِلُوْنَ بِهٖ لَقُضِیَ الْاَمْرُ بَیْنِیْ وَ بَیْنَكُمْ ؕ وَ اللّٰهُ اَعْلَمُ بِالظّٰلِمِیْنَ ﴿۵۹﴾

60. Na ziko Kwake funguo za siri, hakuna azijuaye ila Yeye tu; na Anayajua yaliyomo barani na baharini; na halianguki jani ila Analijua, wala punje katika giza la ardhi; wala kilichorutubika, wala kilichoyabisika, ila yamo katika Kitabu kidhihirishacho.

وَ عِنْدَهٗ مَفَاتِحُ الْغَیْبِ لَا یَعْلَمُهَاۤ اِلَّا هُوَ ؕ وَ یَعْلَمُ مَا فِی الْبَرِّ وَ الْبَحْرِ ؕ وَ مَا تَسْقُطُ مِنْ وَّرَقَةٍ اِلَّا یَعْلَمُهَا وَ لَا حَبَّةٍ فِیْ ظُلُمٰتِ الْاَرْضِ وَ لَا رَطْبٍ وَّ لَا یَابِسٍ اِلَّا فِیْ كِتٰبٍ مُّبِیْنٍ ﴿۶۰﴾

61. Naye ndiye Anayewafisheni wakati wa usiku, na Anayafahamu mnayoyatenda wakati wa mchana, kisha Yeye Huwafufueni humo ili muda uliowekwa umalizike; kisha Kwake ni marudio yenu, ndipo Atawaambieni yale mliyokuwa mkiyafanya

وَ هُوَ الَّذِیْ یَتَوَفّٰىكُمْ بِالَّیْلِ وَ یَعْلَمُ مَا جَرَحْتُمْ بِالنَّهَارِ ثُمَّ یَبْعَثُكُمْ فِیْهِ لِیُقْضٰۤى اَجَلٌ مُّسَمًّى ۚ ثُمَّ اِلَیْهِ مَرْجِعُكُمْ ثُمَّ یُنَبِّئُكُمْ بِمَا كُنْتُمْ تَعْمَلُوْنَ ﴿۶۱﴾ ع ۷ ۴

Aya 61. *Yatawaffaakum billaili,* "Anayewafisheni wakati wa usiku." Mwanachuoni aliyetunga Al-Baharul-Muhit anasema: "Neno tawaffi, ijulikanayo sana maana yake ni 'kufisha', lakini katika Aya hii limetumiwa kwa maana ya 'kulaza usingizi' kwa vile usingizi unavyofanana sana na mauti."

FUNGU 8

وَهُوَ الْقَاهِرُ فَوْقَ عِبَادِهٖ وَيُرْسِلُ
عَلَيْكُمْ حَفَظَةً ؕ حَتّٰٓى اِذَا جَآءَ اَحَدَكُمُ
الْمَوْتُ تَوَفَّتْهُ رُسُلُنَا وَهُمْ لَا يُفَرِّطُوْنَ ﴿٦١﴾

62. Naye ni Mshindi juu ya watu Wake na Huwapelekeeni wahifadhi; hata mmoja wenu anapofikiwa na mauti, Wajumbe Wetu humfisha, nao hawalegei.

ثُمَّ رُدُّوْٓا اِلَى اللّٰهِ مَوْلٰىهُمُ الْحَقِّ ؕ اَلَا لَهُ
الْحُكْمُ ۫ وَهُوَ اَسْرَعُ الْحٰسِبِيْنَ ﴿٦٢﴾

63. Kisha wanarudishwa kwa Allah, Mola wao wa haki. Sikilizeni! Hukumu ni Yake, naye ni Mwepesi wa wanaohesabu.

قُلْ مَنْ يُّنَجِّيْكُمْ مِّنْ ظُلُمٰتِ الْبَرِّ
وَالْبَحْرِ تَدْعُوْنَهٗ تَضَرُّعًا وَّخُفْيَةً ۚ
لَئِنْ اَنْجٰىنَا مِنْ هٰذِهٖ لَنَكُوْنَنَّ
مِنَ الشّٰكِرِيْنَ ﴿٦٣﴾

64. Sema: Ni nani Anayewaokoeni katika taabu za bara na baharini, mnamwomba kwa unyenyekevu na kwa siri: Kama Akituokoa katika hii, bila shaka tutakuwa miongoni mwa wanaoshukuru.

قُلِ اللّٰهُ يُنَجِّيْكُمْ مِّنْهَا وَمِنْ كُلِّ كَرْبٍ
ثُمَّ اَنْتُمْ تُشْرِكُوْنَ ﴿٦٤﴾

65. Sema: Allah Huwaokoeni katika hayo na katika kila mashaka, kisha ninyi mnamshirikisha.

قُلْ هُوَ الْقَادِرُ عَلٰٓى اَنْ يَّبْعَثَ عَلَيْكُمْ
عَذَابًا مِّنْ فَوْقِكُمْ اَوْ مِنْ تَحْتِ اَرْجُلِكُمْ
اَوْ يَلْبِسَكُمْ شِيَعًا وَّيُذِيْقَ بَعْضَكُمْ
بَاْسَ بَعْضٍ ؕ اُنْظُرْ كَيْفَ نُصَرِّفُ
الْاٰيٰتِ لَعَلَّهُمْ يَفْقَهُوْنَ ﴿٦٥﴾

66. Sema: Yeye Ndiye Awezaye kuwaleteeni adhabu kutoka juu yenu au kutoka chini ya miguu yenu, au kusababisha mgawanyike katika vikundi na kuwaonjesheni baadhi yenu mapigano ya wengine. Tazama jinsi Tunavyozieleza Ishara kwa njia mbalimbali ili wapate kufahamu.

وَكَذَّبَ بِهٖ قَوْمُكَ وَهُوَ الْحَقُّ ؕ قُلْ
لَّسْتُ عَلَيْكُمْ بِوَكِيْلٍ ﴿٦٦﴾ ؕ

67. Na watu wako wameikadhibisha, hali hiyo ni haki. Sema: Mimi si mlinzi juu yenu.

لِكُلِّ نَبَاٍ مُّسْتَقَرٌّ ۟ وَّسَوْفَ تَعْلَمُوْنَ ﴿٦٧﴾

68. Kila habari ina wakati maalum, na hivi karibuni ninyi mtajua.

Aya 68. *Naba'*, "Habari." Neno hili hapa mradi wake ni "Bishara." Allah ameweka wakati maalumu wa kutimiza kila bishara, na itakapotimizwa, mtajua.

وَاِذَا رَاَيْتَ الَّذِيْنَ يَخُوْضُوْنَ فِيْۤ اٰيٰتِنَا فَاَعْرِضْ عَنْهُمْ حَتّٰى يَخُوْضُوْا فِيْ حَدِيْثٍ غَيْرِهٖ ؕ وَاِمَّا يُنْسِيَنَّكَ الشَّيْطٰنُ فَلَا تَقْعُدْ بَعْدَ الذِّكْرٰى مَعَ الْقَوْمِ الظّٰلِمِيْنَ ﴿٦٩﴾

69. Na unapowaona wale wanaozifanyia mzaha Aya Zetu, basi ujitenge nao mpaka wazungumze maneno mengine; na kama Shetani akikusahaulisha, basi usikae baada ya kukumbuka pamoja na watu wadhalimu.

وَمَا عَلَى الَّذِيْنَ يَتَّقُوْنَ مِنْ حِسَابِهِمْ مِّنْ شَيْءٍ وَّلٰكِنْ ذِكْرٰى لَعَلَّهُمْ يَتَّقُوْنَ ﴿٧٠﴾

70. Wala si juu ya wale wanaomcha (Allah) hesabu yao (wadhalimu) hata kidogo, lakini ni mawaidha ili wapate kujiepusha.

وَذَرِ الَّذِيْنَ اتَّخَذُوْا دِيْنَهُمْ لَعِبًا وَّلَهْوًا وَّغَرَّتْهُمُ الْحَيٰوةُ الدُّنْيَا وَذَكِّرْ بِهٖۤ اَنْ تُبْسَلَ نَفْسٌۢ بِمَا كَسَبَتْ ۖ لَيْسَ لَهَا مِنْ دُوْنِ اللّٰهِ وَلِيٌّ وَّلَا شَفِيْعٌ ۚ وَاِنْ تَعْدِلْ كُلَّ عَدْلٍ لَّا يُؤْخَذْ مِنْهَا ؕ اُولٰٓئِكَ الَّذِيْنَ اُبْسِلُوْا بِمَا كَسَبُوْا ۚ لَهُمْ شَرَابٌ مِّنْ حَمِيْمٍ وَّعَذَابٌ اَلِيْمٌۢ بِمَا كَانُوْا يَكْفُرُوْنَ ﴿٧١﴾ ع

71. Na uwaache wale walioifanyia dini yao mchezo na upuuzi, na yamewadanganya maisha ya dunia, na uwakumbushe kwayo, isije nafsi yo yote ikaangamizwa kwa sababu ya yale iliyoyachuma. Haina mlinzi wala mwombezi ye yote isipokuwa Allah. Na ingawa itatoa fidia ya kila namna haitapokelewa kwake. Hao ndio walioangamizwa kwa sababu ya yale waliyoyachuma. Wao watapata kinywaji cha maji ya moto na adhabu iumizayo kwa sababu walikuwa wakikataa.

FUNGU 9

قُلْ اَنَدْعُوْا مِنْ دُوْنِ اللّٰهِ مَا لَا يَنْفَعُنَا وَلَا يَضُرُّنَا وَنُرَدُّ عَلٰۤى اَعْقَابِنَا بَعْدَ اِذْ هَدٰىنَا اللّٰهُ كَالَّذِى اسْتَهْوَتْهُ الشَّيٰطِيْنُ فِى الْاَرْضِ حَيْرَانَ ۖ لَهٗۤ اَصْحٰبٌ

72. Sema: Je, tumwombe asiyekuwa Allah ambaye hatufaidishi wala hatudhuru, na turudishwe nyuma baada ya Allah kutuongoza, sawa na yule ambaye mashetani wamemsumbua akiwayawaya katika ardhi? Anao marafiki wanaomwita

Aya 69. Kama watu wanafanyia mzaha Aya za Allah mbele yetu inatakiwa tuondoke mara moja ili wasipate nafasi ya kuendeleza mzaha wao na kujiitia adhabu ya Allah.

Aya 72. Sehemu ya kwanza ya Aya hii inatufunza namna nzuri ya kuhubiri dini; Kwanza

يَّدْعُوْنَهٗۤ اِلَى الْهُدَى ائْتِنَا ؕ قُلْ اِنَّ هُدَى اللّٰهِ هُوَ الْهُدٰى ؕ وَاُمِرْنَا لِنُسْلِمَ لِرَبِّ الْعٰلَمِيْنَ ۙ﴿۷۱﴾

kwenye mwongozo (wakisema): Njoo kwetu. Sema: Mwongozo hasa ni mwongozo wa Allah, na tumeamrishwa tujisalimishe kwa Mola wa walimwengu wote.

وَاَنْ اَقِيْمُوا الصَّلٰوةَ وَاتَّقُوْهُ ؕ وَهُوَ الَّذِيْۤ اِلَيْهِ تُحْشَرُوْنَ ﴿۷۲﴾

73. Na kasimamisheni Sala na Mcheni Yeye; Naye ndiye Ambaye mtakusanywa Kwake.

وَهُوَ الَّذِيْ خَلَقَ السَّمٰوٰتِ وَالْاَرْضَ بِالْحَقِّ ؕ وَيَوْمَ يَقُوْلُ كُنْ فَيَكُوْنُ ۬ؕ قَوْلُهُ الْحَقُّ ؕ وَلَهُ الْمُلْكُ يَوْمَ يُنْفَخُ فِي الصُّوْرِ ؕ عٰلِمُ الْغَيْبِ وَالشَّهَادَةِ ؕ وَهُوَ الْحَكِيْمُ الْخَبِيْرُ ﴿۷۳﴾

74. Naye Ndiye Aliyeziumba mbingu na ardhi kwa haki; na siku Atakaposema; 'kuwa, basi huwa'. Kauli Yake ni haki, na ufalme ni wake siku itakapopulizwa parapanda; Mjuzi wa siri na dhahiri; naye ndiye Mwenye hekima, Mwenye habari.

وَاِذْ قَالَ اِبْرٰهِيْمُ لِاَبِيْهِ اٰزَرَ اَتَتَّخِذُ اَصْنَامًا اٰلِهَةً ۚ اِنِّيْۤ اَرٰىكَ وَقَوْمَكَ فِيْ ضَلٰلٍ مُّبِيْنٍ ﴿۷۴﴾

75. Na (kumbukeni) Ibrahimu alipomwambia baba yake, Azar; Je, unashika masananu kuwa miungu? Hakika ninakuona wewe na watu wako katika upotevu dhahiri.

وَكَذٰلِكَ نُرِيْۤ اِبْرٰهِيْمَ مَلَكُوْتَ السَّمٰوٰتِ وَالْاَرْضِ وَلِيَكُوْنَ مِنَ الْمُوْقِنِيْنَ ﴿۷۵﴾

76. Na hivyo Tukamwonyesha Ibrahimu ufalme wa mbingu na ardhi, na ili awe miongoni mwa wenye yakini.

---

kubainisha makosa ya wapinzani kama inavyoashiriwa na maneno haya *hatufaidishi wala hatudhuru;* kisha kueleza ukweli kama inavyoashiriwa na maneno haya, *baada ya Allah kutuongoza.*

Aya 74. Maneno *kun fayakuun* 'kuwa basi huwa' hayaonyeshi mabadiliko yanayojileta yenyewe kutoka katika hali ya kutokuwepo kitu kuja katika hali ya kuwepo kwa kitu. Yana maana kwamba mara Allah Anapotaka, ule utashi Wake unaanza kuchukua sura na mwishowe hufanyika kama Anavyokusudia.

Aya 75. *Ab,* "Baba." Neno hili pia lina maana hizi, babu; ndugu wa baba. Azar hakuwa baba mzazi wa Nabii Ibrahimu, bali alikuwa ndugu wa baba yake. sababu ni hii. Nabii Ibrahimu aliweka ahadi ya kumwombea *ab* yake aitwaye Azar ambaye alikuwa mchonga miungu ya masanamu. Alipojua kuwa huyo *ab* yake ni adui wa Allah aliachilia mbali kumwombea. Lakini katika siku za mwisho za maisha yake Nabii Ibrahimu alipojenga Kaaba pamoja na mwanawe Ismail, alimwombea *waalid* (baba mzazi) wake, na hakukatazwa kumwombea. Hii inaonyesha ya kuwa baba mzazi wa Ibrahimu ni mtu mwingine na Azar alikuwa ndugu wa baba yake tu.

Aya 76. *Malakuut.* "Ufalme." Neno hili maana yake ni enzi, milki, ufalme mkubwa, uwezo wa kukifanyia kitu kama atakavyo, mahali pa roho takatifu mbinguni (Akrab). Neno

فَلَمَّا جَنَّ عَلَيْهِ الَّيْلُ رَاٰ كَوْكَبًا ۚ قَالَ هٰذَا رَبِّيْ ۚ فَلَمَّآ اَفَلَ قَالَ لَآ اُحِبُّ الْاٰفِلِيْنَ ﴿٧٧﴾

77. Na usiku ulipomfikia akaiona nyota, akanena: Hii ni Mola wangu? Lakini ilipotua, akasema: Sipendi vituavyo.

فَلَمَّا رَاَ الْقَمَرَ بَازِغًا قَالَ هٰذَا رَبِّيْ ۚ فَلَمَّآ اَفَلَ قَالَ لَئِنْ لَّمْ يَهْدِنِيْ رَبِّيْ لَاَكُوْنَنَّ مِنَ الْقَوْمِ الضَّآلِّيْنَ ﴿٧٨﴾

78. Na alipouona mwezi unang'aa, akasema: Huu ni Mola wangu? Lakini ulipotua, akasema: Asingaliniongoza Mola wangu, bila shaka ningalikuwa miongoni mwa watu wapotevu.

فَلَمَّا رَاَ الشَّمْسَ بَازِغَةً قَالَ هٰذَا رَبِّيْ هٰذَآ اَكْبَرُ ۚ فَلَمَّآ اَفَلَتْ قَالَ يٰقَوْمِ اِنِّيْ بَرِيْٓءٌ مِّمَّا تُشْرِكُوْنَ ﴿٧٩﴾

79. Na alipoliona jua linang'aa, akasema: Hili ni Mola wangu? Hili kubwa kabisa! Lakini lilipotua akasema: Enyi watu wangu! mimi simo katika hayo mnayoyashirikisha.

اِنِّيْ وَجَّهْتُ وَجْهِيَ لِلَّذِيْ فَطَرَ السَّمٰوٰتِ وَالْاَرْضَ حَنِيْفًا وَّمَآ اَنَا مِنَ الْمُشْرِكِيْنَ ﴿٨٠﴾

80. Kwa yakini mimi nimejielekeza uso wangu kwa Yule Aliyeziumba mbingu na ardhi, kwa kujihalisisha, tena mimi si miongoni mwa washirikina.

وَحَآجَّهٗ قَوْمُهٗ ۚ قَالَ اَتُحَآجُّوْٓنِّيْ فِي اللّٰهِ وَقَدْ هَدٰىنِ ۚ وَلَآ اَخَافُ مَا تُشْرِكُوْنَ بِهٖٓ

81. Na watu wake wakajadiliana naye, Akasema, Je, mnanihoji juu ya Allah na hali Yeye Ameniongoza? Wala siviogopi vile

---

Malakuut hasa hutumika kwa kutaja ufalme au milki ya Allah (Mufradat).

Maneno haya, *Tukamwonyesha Ibrahimu ufalme wa mbingu,* maana yake, Tulimwonyesha Ibrahimu uwezo na mamlaka Tuliyo nayo, juu ya kila sehemu ya ulimwengu. Walii mkubwa wa Kiislamu aitwaye Shihabuddin Suhrwardi, ameandika katika kitabu chake maarufu kiitwacho "'Awaariful-Ma'aarif" ya kwamba msafiri wa kiroho, anapofikia daraja hii, yaani anapowezeshwa kuiona enzi ya Allah anakuwa kama ilivyo, anayezaliwa tena kiroho, na ya kwamba hakuna mtu anayeweza kupelekwa mbele ya Allah mpaka amefikia daraja hii ya yakini. Lakini mtu anapofikia daraja hii ya yakini, wasiwasi hauwezi kupenya ndani ya moyo wake, kwani hapo atakuwa anaishi mbele hasa ya Allah.

Aya 77, 78, 79. Watu wengine wanadhani ya kuwa Nabii Ibrahimu alipata kusadiki ya kuwa nyota na jua na mwezi ni miungu, na alipoona vinatua ndipo akavikataa. Hivi sivyo. Hapa Nabii Ibrahimu alikuwa anashindana na watu wake na akatumia njia hiyo ya usemi ili kuwafahamisha makosa yao. Ni kama kuwaambia, Je, mnasema hili jua na mwezi na nyota kuwa miungu wangu? Mbona vinatoka na kutoweka? Vitu vya namna hii haviwezi kuwa Mungu.

Aya 80, 81, 82. Aya hizi zinahakikisha kuwa Nabii Ibrahimu alikuwa anamwamini Allah na akizijua sana sifa Zake, na hii yote ilikuwa anafanya bidii kuwavuta pole pole watu wake kwa Allah.

mnavyomshrikisha naye,isipokuwa Mola wangu akipenda cho chote. Mola wangu Anao wasaa wa elimu ya kila kitu; basi je hamshiki mawaidha?

اِلَّاۤ اَنۡ يَّشَآءَ رَبِّىۡ شَيۡـئًا ؕ وَسِعَ رَبِّىۡ كُلَّ شَىۡءٍ عِلۡمًا ؕ اَفَلَا تَتَذَكَّرُوۡنَ ﴿۸۰﴾

82. Na nitaogopaje hayo mnayooyashirikisha , hali ninyi hamuogopi kumshirikisha Allah na kile ambacho hakukiteremshia dalili kwenu? Basi kundi gani katika mawili linastahili zaidi kupata amani, ikiwa ninyi mnajua?

وَكَيۡفَ اَخَافُ مَاۤ اَشۡرَكۡتُمۡ وَلَا تَخَافُوۡنَ اَنَّكُمۡ اَشۡرَكۡتُمۡ بِاللّٰهِ مَا لَمۡ يُنَزِّلۡ بِهٖ عَلَيۡكُمۡ سُلۡطٰنًا ؕ فَاَىُّ الۡفَرِيۡقَيۡنِ اَحَقُّ بِالۡاَمۡنِ ۚ اِنۡ كُنۡتُمۡ تَعۡلَمُوۡنَ ﴿۸۱﴾

83. Wale walioamini na hawakuchanganya imani yao na dhuluma, hao ndio ambao watapata amani, nao ndio wanaoongozwa.

اَلَّذِيۡنَ اٰمَنُوۡا وَلَمۡ يَلۡبِسُوۡۤا اِيۡمَانَهُمۡ بِظُلۡمٍ اُولٰٓئِكَ لَهُمُ الۡاَمۡنُ وَهُمۡ مُّهۡتَدُوۡنَ ﴿۸۲﴾

FUNGU 10

84. Na hiyo ndio hoja Yetu Tuliyompa Ibrahimu juu ya watu wake. Tunamnyanyua katika vyeo yule Tumtakaye; hakika Mola wako ndiye Mwenye hekima, Ajuaye.

وَتِلۡكَ حُجَّتُنَاۤ اٰتَيۡنٰهَاۤ اِبۡرٰهِيۡمَ عَلٰى قَوۡمِهٖ ؕ نَرۡفَعُ دَرَجٰتٍ مَّنۡ نَّشَآءُ ؕ اِنَّ رَبَّكَ حَكِيۡمٌ عَلِيۡمٌ ﴿۸۳﴾

85. Na Tukampa Isihaka na Yakubu; wote Tukawaongoza, na Nuhu Tulimwongoza zamani, na katika wazao wake, Daudi na Suleimani na Ayubu na Yusuf na Musa na Harun; na hivi ndivyo Tuwalipavyo wafanyao hisani:

وَوَهَبۡنَا لَهٗۤ اِسۡحٰقَ وَيَعۡقُوۡبَ ؕ كُلًّا هَدَيۡنَا ۚ وَنُوۡحًا هَدَيۡنَا مِنۡ قَبۡلُ وَمِنۡ ذُرِّيَّتِهٖ دَاوٗدَ وَسُلَيۡمٰنَ وَاَيُّوۡبَ وَيُوۡسُفَ وَمُوۡسٰى وَهٰرُوۡنَ ؕ وَكَذٰلِكَ نَجۡزِى الۡمُحۡسِنِيۡنَ ﴿۸۴﴾

86. Na Zakaria na Yahya na Isa na Ilyasa; wote walikuwa miongoni mwa watu wema.

وَزَكَرِيَّا وَيَحۡيٰى وَعِيۡسٰى وَاِلۡيَاسَ ؕ كُلٌّ مِّنَ الصّٰلِحِيۡنَ ﴿۸۵﴾

87. Na Ismaili na Elisha na Yunus na Luti, na wote Tukawafadhili juu ya walimwengu.

وَاِسۡمٰعِيۡلَ وَالۡيَسَعَ وَيُوۡنُسَ وَلُوۡطًا ؕ وَكُلًّا فَضَّلۡنَا عَلَى الۡعٰلَمِيۡنَ ﴿۸۶﴾

Aya 85 - 87. Katia Aya hizi majina ya Manabii yamewekwa katika mpango wa hekima sana ulio mzuri. Ni vigumu makafiri kuifahamu Qur'an vizuri kwa sababu ya giza liliomo mioyoni mwao la uadui. Sasa hapa pia tutadhihirisha ujinga mwingine wa Padre Dale. Sikieni anavyosema juu ya Aya hizi. Ameandika, "Majina ya Manabii hawa yanatajwa ovyo tu. Ishmael hatajwi kabla

ya Isaaka; na baada ya kumtaja Nuhu, amtia Daud na Suleimani, katika wazao wake Nuhu, akirukiza wengi . . . . Tena amtia Eliya pamoja na Zakaria na Yohana mbatizaji na Bwana wetu . . . ni kana kwamba ataja kila mmoja alikumbukapo jina lake bila kufikiri wakati alipokuwako duniani" (uk. 589 590).

MPANGO WA QUR'AN UNA HEKIMA.

Kupanga majina kama watu walivyofuatana katika kuzaliwa ndio elimu moja aliyoijua Padre Dale. Akiwakuta watu wamewekwa mahali, mara anaona aliyesimama mbele yao ndiye wa kwanza kuzaliwa! Kama Qur'an ingesema mpango wa Manabii hao katika Aya hiyo ndivyo walivyofuatana katika kuja duniani, Padre Dale angekuwa na haki ya kuleta lawama. Lakini Qur'an haikusema hivyo. Ukitazama Aya hizo tatu, mara utaona kuwa kuna mpango maalumu uliokusudiwa. Manabii wa Aya ya mbele wameitwa *Al-Muhsiniin,* waliotajwa katika Aya ya pili yake wameitwa *Assaalihiin*, na wa Aya ya tatu wamesemwa, *Fadhdhalnaa 'alal-'aalamiin*. Wamepangwa kama vile vikosi vya watu wenye kazi au sifa mbalimbali. Hivyo, kama kusudio ni hilo la kuwaonyesha kila kundi waliofanana pamoja, ingekuwa maana gani kuwapanga kwa kufuata tarehe za kufika kwao? Je, mnaona ulivyo werevu wa Padre Dale!

Aya hizi tatu zinaonyesha ya kwamba si Ibrahimu tu aliyehubiri kuilaumu shirki, bali Manabii wengine pia.

Aya 85 inataja wazao wa Ibrahimu mpaka kizazi cha pili, ikimtaja mtoto wa Ibrahimu (Isihaka) na mjukuu wake (Yakubu au Israeli). Jina la Ismaili linatajwa katika fungu jingine asiwekwe katika daraja dogo la kuwa chini ya Ibrahimu.

KUNDI LA KWANZA

Utaona ya kuwa Manabii waliotokana na Nuhu katika Aya hizi tatu wamegawanywa katika mafungu matatu. Fungu la kwanza lina Daudi, Suleimani, Ayubu, Yusuf, Musa na Harun, ambao ni Manabii waliopewa mamlaka, mali na ustawi, na hivyo wakaweza kuwatendea wema wanadamu. Hivyo Manabii wa kundi hili wameitwa *Al-Muhsiniin*, yaani, wafanyao hisani. Daudi na Suleimani walikuwa wafalme. Yusuf na Ayubu walipewa ustawi baada ya kujaribiwa kwa mateso na kuonyesha subira kubwa. Musa na Harun walifaidi mamlaka makubwa kati ya watu wao.

KUNDI LA PILI.

Kundi la pili limetajwa katika Aya 86, nao ni Zakaria, Yahya, Isa na Ilyasa. Hakuna ye yote katika hawa aliyepata mamlaka ya kidunia au mali, wote waliishi maisha ya unyonge na ya chini, hata inasemwa ya kuwa Ilyasa alikuwa akionekana kwa nadra tu na akiishi porini. Kwa sababu hii kundi hili limetajwa pa peke yake, nao wameitwa *Assaalihiin,* yaani watu wema, watawa. Watatu wa kwanza katika hili kundi la pili walifuatana; na ingawa Ilyasa si wa majira moja nao, alifanana sana na Yahya (Yohana) ambaye alikuja katika jinsi na nguvu ya Iyasa (Eliya), (kama alivyosema Yesu, kuwajibu wanafunzi wake, "Eliya yuaja kwanza, nae atatengeneza yote; lakini nawaambieni, ya kwamba Eliya amekwisha kuja, wasimtambue, wakamtendea yote waliyotaka . . . Ndipo wakafahamu wale wanafunzi ya kuwa amesema nao habari za Yohana Mbatizaji (Mat. 17:10-13); hivyo Ilyasa naye ametiwa ndani ya kundi hilo.

KUNDI LA TATU

Kundi la tatu linatajwa katika Aya 87, nao ni Ismaili, Elisha, Yunus na Luti. Hawa hawakuwa na mamlaka ya kidunia, lakini Allah aliwapa fadhili na ubora. Hawa wamesingiziwa ya kwamba walikuwa na tamaa ya kupata mamlaka na utajiri.

Juu ya Ismaili, tunasoma katika Biblia, "Atakuwa mfano wa punda wa mwitu kati ya wanadamu; mkono wake utakuwa kinyume cha kila mtu, na kila mtu vivyo atakuwa ni kinyume

وَمِنْ اٰبَآىِٕهِمْ وَذُرِّيّٰتِهِمْ وَاِخْوَانِهِمْ ۚ وَاجْتَبَيْنٰهُمْ وَهَدَيْنٰهُمْ اِلٰى صِرَاطٍ مُّسْتَقِيْمٍ ﴿٨٨﴾

88. Na katika baba zao na wazao wao na ndugu zao, na tukawachagua na tukawaongoza kwenye njia iliyonyooka.

ذٰلِكَ هُدَى اللّٰهِ يَهْدِىْ بِهٖ مَنْ يَّشَآءُ مِنْ عِبَادِهٖ ؕ وَلَوْ اَشْرَكُوْا لَحَبِطَ عَنْهُمْ مَّا كَانُوْا يَعْمَلُوْنَ ﴿٨٩﴾

89. Huo ni mwongozo wa Allah. Kwa huo Humwongoza Amtakaye katika watu Wake. Na kama wangemshirikisha (Allah), bila shaka yangaliwaharibikia yale waliyokuwa wakiyatenda.

اُولٰٓئِكَ الَّذِيْنَ اٰتَيْنٰهُمُ الْكِتٰبَ وَالْحُكْمَ وَالنُّبُوَّةَ ۚ فَاِنْ يَّكْفُرْ بِهَا هٰٓؤُلَآءِ فَقَدْ وَكَّلْنَا بِهَا قَوْمًا لَّيْسُوْا بِهَا بِكٰفِرِيْنَ ﴿٩٠﴾

90. Hao ndio Tuliowapa Kitabu na hukumu na utume; kwa hiyo kama hawa wakiyakataa hayo, basi Tumekwisha yawekea watu wasioyakataa.

اُولٰٓئِكَ الَّذِيْنَ هَدَى اللّٰهُ فَبِهُدٰىهُمُ اقْتَدِهْ ؕ قُلْ لَّآ اَسْـَٔلُكُمْ عَلَيْهِ اَجْرًا ؕ اِنْ هُوَ اِلَّا ذِكْرٰى لِلْعٰلَمِيْنَ ﴿٩١﴾ ع

91. Hao ndio ambao Allah Amewaongoza, basi ufuate mwongozo wao. Sema: Siwaombeni ujira juu ya hayo; siyo haya ila ni mawaidha kwa watu.

---

chake" (Mwanzo 16:12). Katika Talmud, Ismaili anasemwa ya kuwa alimfuata baba yake Ibrahimu wakati Ibrahimu alipotoka na Isihaka kwenda mchinja(Isihaka) kama dhabihu, akifurahi kuwa amebaki peke yake kurithi mashamba yote na makundi yote ya wanyama.

Elisha anasemwa kuwa alimwulisha mfalme aliyekataa kumtii ili yeye apate kuwa na nguvu katika mambo ya utawala.

Yunus anasemwa alimkasirikia Mungu kwa kuwa aliaibishwa kwa sababu bishara aliyotoa haikutimia, na ya kwamba alitafuta kupata utawala.

Luti anasemwa ya kuwa alifanyia tamaa sana ardhi za malisho zenye rutuba na ya kwamba siku zote alikuwa akigombana na ami yake, Ibrahimu .

Hivyo Manabii hawa wamelaumiwa na watu kwamba walikuwa ni wenye tamaa sana ya mali na mamlaka. Lakini Qur'an inatangaza ya kwamba lawama hizo zote ni za uwongo, na ya kwamba hao Manabii walifadhiliwa cheo cha juu kuliko watu wengine.

MPANGO HUU NDIO BORA

Ni wazi kabisa mpango waliopangwa Manabii hao katika Aya hizo ni wa maana sana na bora, tena wenye hekima kweli-kweli, na hakuna mpango mwingine wo wote ungeweza kuwa bora ya huo. Manabii wenye hali zinazofanana wamewekwa kifungu kimoja ili kuonyesha namna na fadhili mbalimbali za Allah walizopewa; na waliolaumiwa, kusafishwa na lawama hizo. Siyo wazi mashtaka ya Padre Dale yanathibitisha kuwa yeye mwenyewe ndiye anayejisemea "ovyo." Kuna methali isemayo "Chura aliyomo kisimani atajuaje yaliyoko baharini!"

FUNGU 11

92. Na walishindwa kumheshimu Allah kama ilivyotakiwa kumheshimu pale waliposema: Allah Hakuteremsha cho chote juu ya binadamu. Sema: Ni nani Aliyekiteremsha Kitabu alicholeta Musa, chenye nuru na mwongozo kwa watu, mlichokifanya nyaraka nyaraka, mkadhihirisha sehemu yake na yaliyo mengi mkayaficha? Na mkafundishwa msiyoyajua ninyi wala baba zenu. Sema: Allah (ndiye Aliyekiteremsha); kisha waache wacheze katika porojo yao.

وَمَا قَدَرُوا اللّٰهَ حَقَّ قَدْرِهٖۤ اِذْ قَالُوْا مَاۤ اَنْزَلَ اللّٰهُ عَلٰى بَشَرٍ مِّنْ شَیْءٍ ؕ قُلْ مَنْ اَنْزَلَ الْكِتٰبَ الَّذِیْ جَآءَ بِهٖ مُوْسٰى نُوْرًا وَّهُدًى لِّلنَّاسِ تَجْعَلُوْنَهٗ قَرَاطِیْسَ تُبْدُوْنَهَا وَ تُخْفُوْنَ كَثِیْرًا ۚ وَعُلِّمْتُمْ مَّا لَمْ تَعْلَمُوْۤا اَنْتُمْ وَلَاۤ اٰبَآؤُكُمْ ؕ قُلِ اللّٰهُ ۙ ثُمَّ ذَرْهُمْ فِیْ خَوْضِهِمْ یَلْعَبُوْنَ ﴿۹۱﴾

93. Na hiki ni Kitabu Tulichokiteremsha, kilichobarikiwa, kinasadikisha yale yaliyokitangulia, na ili uuonye Mama wa miji na walio pembezoni mwake. Na wale wanaoiamini Akhera hukisadiki, nao huzihifadhi Sala zao.

وَهٰذَا كِتٰبٌ اَنْزَلْنٰهُ مُبٰرَكٌ مُّصَدِّقُ الَّذِیْ بَیْنَ یَدَیْهِ وَلِتُنْذِرَ اُمَّ الْقُرٰى وَمَنْ حَوْلَهَا ؕ وَالَّذِیْنَ یُؤْمِنُوْنَ بِالْاٰخِرَةِ یُؤْمِنُوْنَ بِهٖ وَهُمْ عَلٰى صَلَاتِهِمْ یُحَافِظُوْنَ ﴿۹۲﴾

94. Na ni nani mdhalimu mkubwa kuliko yule Amtungiaye uwongo Allah au mwenye kusema: Nimefunuliwa na hali hakufunuliwa cho chote, na yule asemaye: Hivi karibuni nitateremsha (ufunuo) kama ule Aliouteremsha Allah? Na kama ungewaona wadhalimu wataka pokuwa katika mahangaiko ya mauti na Malaika watakapoinyoosha mikono yao (na kuwaambia): Zitoeni roho zenu; leo mtalipwa adhabu ifedheheshayo kwa sababu ya yale mliyokuwa mkisema juu ya Allah pasipo haki, na mlikuwa mkizifanyia kiburi Aya Zake.

وَمَنْ اَظْلَمُ مِمَّنِ افْتَرٰى عَلَى اللّٰهِ كَذِبًا اَوْ قَالَ اُوْحِیَ اِلَیَّ وَلَمْ یُوْحَ اِلَیْهِ شَیْءٌ وَّمَنْ قَالَ سَاُنْزِلُ مِثْلَ مَاۤ اَنْزَلَ اللّٰهُ ؕ وَلَوْ تَرٰۤى اِذِ الظّٰلِمُوْنَ فِیْ غَمَرٰتِ الْمَوْتِ وَالْمَلٰٓئِكَةُ بَاسِطُوْۤا اَیْدِیْهِمْ ۚ اَخْرِجُوْۤا اَنْفُسَكُمْ ؕ اَلْیَوْمَ تُجْزَوْنَ عَذَابَ الْهُوْنِ بِمَا كُنْتُمْ تَقُوْلُوْنَ عَلَى اللّٰهِ غَیْرَ الْحَقِّ وَكُنْتُمْ عَنْ اٰیٰتِهٖ تَسْتَكْبِرُوْنَ ﴿۹۳﴾

95. Na bila shaka ninyi mmetujia mmoja mmoja kama Tulivyowaumbeni mara ya kwanza na mmeyaacha nyuma yenu Tuliyowapeni, na Hatuwaoni waombezi wenu pamoja nanyi ambao mlidai kuwa ni washirika (wa Allah) kwenu. Kwa hakika yamekatika (mahusiano yaliyokuwa) baina yenu, na yamewapoteeni mliyokuwa mkidai.

وَلَقَدْ جِئْتُمُوْنَا فُرَادٰى كَمَا خَلَقْنٰكُمْ
اَوَّلَ مَرَّةٍ وَّتَرَكْتُمْ مَّا خَوَّلْنٰكُمْ وَرَآءَ
ظُهُوْرِكُمْ ۚ وَمَا نَرٰى مَعَكُمْ
شُفَعَآءَكُمُ الَّذِيْنَ زَعَمْتُمْ اَنَّهُمْ فِيْكُمْ
شُرَكٰٓؤُا ؕ لَقَدْ تَّقَطَّعَ بَيْنَكُمْ وَضَلَّ
عَنْكُمْ مَّا كُنْتُمْ تَزْعُمُوْنَ ﴿۹۵﴾ ع ۱۱

FUNGU 12

96. Bila shaka Allah ndiye Mchipushaji wa mbegu na kokwa. Hutoa mzima katika maiti, naye ni Mtoaji wa maiti katika mzima. Huyo ndiye Allah; basi mnageuzwa wapi?

اِنَّ اللّٰهَ فَالِقُ الْحَبِّ وَالنَّوٰى ؕ يُخْرِجُ
الْحَيَّ مِنَ الْمَيِّتِ وَمُخْرِجُ الْمَيِّتِ مِنَ
الْحَيِّ ؕ ذٰلِكُمُ اللّٰهُ فَاَنّٰى تُؤْفَكُوْنَ ﴿۹۶﴾

97. Ndiye Aichipushaye asubuhi; na Ameufanya usiku kuwa starehe, na jua na mwezi kwa kuhesabu. Huo ndio mpimo wa Mwenye nguvu, Ajuaye.

فَالِقُ الْاِصْبَاحِ ۚ وَجَعَلَ الَّيْلَ سَكَنًا
وَّالشَّمْسَ وَالْقَمَرَ حُسْبَانًا ؕ ذٰلِكَ
تَقْدِيْرُ الْعَزِيْزِ الْعَلِيْمِ ﴿۹۷﴾

98. Na Yeye ndiye Aliyewafanyieni nyota ili mwongoke kwazo katika giza za bara na baharini; hakika Tumezieleza Aya kwa watu wanaojua.

وَهُوَ الَّذِيْ جَعَلَ لَكُمُ النُّجُوْمَ لِتَهْتَدُوْا
بِهَا فِيْ ظُلُمٰتِ الْبَرِّ وَالْبَحْرِ ؕ قَدْ فَصَّلْنَا
الْاٰيٰتِ لِقَوْمٍ يَّعْلَمُوْنَ ﴿۹۸﴾

99. Na Yeye ndiye Aliyewaumbeni katika nafsi moja, na pako (kwa ajili yenu) mahali pa kukaa kwa muda na mahali pa kukaa milele: hakika Tumezieleza Aya kwa watu wanaofahamu.

وَهُوَ الَّذِيْٓ اَنْشَاَكُمْ مِّنْ نَّفْسٍ وَّاحِدَةٍ
فَمُسْتَقَرٌّ وَّ مُسْتَوْدَعٌ ؕ قَدْ فَصَّلْنَا
الْاٰيٰتِ لِقَوْمٍ يَّفْقَهُوْنَ ﴿۹۹﴾

Aya 96. *Mchipushaji wa mbegu na kokwa,* yaani kama vile mbegu na kokwa zinachipuka na kuwa miti mikubwa, kadhalika mwanadamu amefanana na mbegu, na amekusudiwa kuwa kitu kitukufu.

Humtoa aliye hai katika mfu, ni maneno yanayoweza kufasiriwa namna nyingi. Inawezekana watoto wa watu waovu wawe watu wema, maana watu waovu ni wafu wa kiroho.

Aya 97. *Ndiye Azichipushaye asubuhi,* yaani kama vile Allah anavyoleta mapambazuko na kuufanya usiku ubadilike uwe mchana, vivyo hivyo huwatoa watu katika giza la kiroho na kuwatia katika nuru. Huwatoa katika giza la kufuru na kuwaingiza katika nuru ya imani na wema.

وَهُوَ الَّذِیۡۤ اَنۡزَلَ مِنَ السَّمَآءِ مَآءً ۚ فَاَخۡرَجۡنَا بِهٖ نَبَاتَ كُلِّ شَیۡءٍ فَاَخۡرَجۡنَا مِنۡهُ خَضِرًا نُّخۡرِجُ مِنۡهُ حَبًّا مُّتَرَاكِبًا ۚ وَمِنَ النَّخۡلِ مِنۡ طَلۡعِهَا قِنۡوَانٌ دَانِیَةٌ وَّجَنّٰتٍ مِّنۡ اَعۡنَابٍ وَّالزَّیۡتُوۡنَ وَالرُّمَّانَ مُشۡتَبِهًا وَّغَیۡرَ مُتَشَابِهٍ ؕ اُنۡظُرُوۡۤا اِلٰی ثَمَرِهٖۤ اِذَاۤ اَثۡمَرَ وَیَنۡعِهٖ ؕ اِنَّ فِیۡ ذٰلِكُمۡ لَاٰیٰتٍ لِّقَوۡمٍ یُّؤۡمِنُوۡنَ ﴿۱۰۰﴾

100. Na Yeye ndiye Aliyeteremsha maji kutoka mawinguni, na kwayo Tunaotesha mimea ya kila kitu, kisha tunachipusha majani ya kijani katika hiyo; Tunatokeza katika hiyo punje zilizopangana; na katika mitende (Tunatokeza) katika makole yake vishada vyenye kuinama karibu karibu, na bustani za mizabibu na zaituni na makomamanga, yanayofanana na yasiyofanana. Angalieni matunda yake yanapopamba na kuiva kwake. Bila shaka katika hayo ziko Ishara kwa watu wanaoamini.

وَجَعَلُوۡا لِلّٰهِ شُرَكَآءَ الۡجِنَّ وَخَلَقَهُمۡ وَخَرَقُوۡا لَهٗ بَنِیۡنَ وَبَنٰتٍۢ بِغَیۡرِ عِلۡمٍ ؕ سُبۡحٰنَهٗ وَتَعٰلٰی عَمَّا یَصِفُوۡنَ ﴿۱۰۱﴾ ع ۱۲

101. Na wakamfanyia Allah majinni kuwa washirika, hali Yeye Amewaumba. Na wanamsingizia kuwa na wana wa kiume na wa kike pasipo kujua. Ameepukana na upungufu, na Yu juu kuliko yale wanayomsifu nayo.

FUNGU 13

بَدِیۡعُ السَّمٰوٰتِ وَالۡاَرۡضِ ؕ اَنّٰی یَكُوۡنُ لَهٗ وَلَدٌ وَّلَمۡ تَكُنۡ لَّهٗ صَاحِبَةٌ ؕ وَخَلَقَ كُلَّ شَیۡءٍ ۚ وَهُوَ بِكُلِّ شَیۡءٍ عَلِیۡمٌ ﴿۱۰۲﴾

102. Mwanzishaji wa mbingu na ardhi! Inamkinikaje Awe na mwana hali hana mke, naye Aliumba kila kitu naye ni Mjuzi wa kila kitu?

ذٰلِكُمُ اللّٰهُ رَبُّكُمۡ ۚ لَاۤ اِلٰهَ اِلَّا هُوَ ۚ خَالِقُ كُلِّ شَیۡءٍ فَاعۡبُدُوۡهُ ۚ وَهُوَ عَلٰی كُلِّ شَیۡءٍ وَّكِیۡلٌ ﴿۱۰۳﴾

103. Huyo ndiye Allah , Mola wenu, hakuna aabudiwaye ila Yeye, Mwumba wa kila kitu, kwa hiyo Mwabuduni; naye ni Mlinzi wa kila kitu.

Aya 102. Baada ya kueleza mafundisho yaliyobuniwa na watu, Qur'an imeanza kueleza mafundisho ya Kiungu.

Mtu anaweza kupata mtoto kwa njia mbili tu. Ama kwa kuwa na mke au kwa kumpanga. Kwa njia ya kwanza, Mungu hana mke, hivyo hawezi kuwa na mwana. Wakristo wanamwita Yesu mwana wa Mungu, lakini hawamwiti Mariamu mke wa Mungu. Basi, kama Yesu alikuwa ni mwana wa Mungu wa kupanga tu, hilo halitompa ubora kuliko wanadamu wengine, maana mtu mwingine ye yote angeweza kupangwa utoto na Allah. Isitoshe, kwa kuwa Allah ni Mwumba wa kila kitu, ana ujuzi kamili, hana haja ya kuwa na mwana.

لَا تُدْرِكُهُ الْاَبْصَارُ ۖ وَهُوَ يُدْرِكُ
الْاَبْصَارَ ۚ وَهُوَ اللَّطِيْفُ الْخَبِيْرُ ﴿١٠٣﴾

104. Macho Hayamfikii, bali Yeye Anayafikia Macho; naye ni Latifu, Mwenye habari.

قَدْ جَآءَكُمْ بَصَآئِرُ مِنْ رَّبِّكُمْ ۚ فَمَنْ
اَبْصَرَ فَلِنَفْسِهٖ ۚ وَمَنْ عَمِيَ فَعَلَيْهَا ؕ
وَمَآ اَنَا عَلَيْكُمْ بِحَفِيْظٍ ﴿١٠٤﴾

105. Hakika zimewafikieni hoja zenye busara kutoka kwa Mola wenu, basi anayeona ni kwa faida yake mwenyewe, na anayepofuka, basi ni kwa hasara yake mwenyewe; nami si mhifadhi wenu.

وَكَذٰلِكَ نُصَرِّفُ الْاٰيٰتِ وَلِيَقُوْلُوْا
دَرَسْتَ وَلِنُبَيِّنَهٗ لِقَوْمٍ يَّعْلَمُوْنَ ﴿١٠٥﴾

106. Na hivi ndivyo Twazikariri Aya kwa namna mbali mbali (wapate kufahamu) ili wapate kusema umejifunza sana na kufundisha barabbara na ili Tubainishe vyema kwa watu wanaojua.

اِتَّبِعْ مَآ اُوْحِيَ اِلَيْكَ مِنْ رَّبِّكَ ۚ لَآ اِلٰهَ
اِلَّا هُوَ ۚ وَاَعْرِضْ عَنِ الْمُشْرِكِيْنَ ﴿١٠٦﴾
وَلَوْ شَآءَ اللّٰهُ مَآ اَشْرَكُوْا ؕ وَمَا جَعَلْنٰكَ
عَلَيْهِمْ حَفِيْظًا ۚ وَمَآ اَنْتَ عَلَيْهِمْ
بِوَكِيْلٍ ﴿١٠٧﴾

107. Ufuate uliyofunuliwa kutoka kwa Mola wako, hakuna aabudiwaye ila Yeye: na ujitenge na washirikina.

108. Na kama Allah Angependa wasingalishirikisha; na Sisi Hatukukufanya uwe mhifadhi juu yao, wala wewe si mlinzi wao.

وَلَا تَسُبُّوا الَّذِيْنَ يَدْعُوْنَ مِنْ دُوْنِ اللّٰهِ
فَيَسُبُّوا اللّٰهَ عَدْوًاۢ بِغَيْرِ عِلْمٍ ؕ كَذٰلِكَ
زَيَّنَّا لِكُلِّ اُمَّةٍ عَمَلَهُمْ ۪ ثُمَّ اِلٰى رَبِّهِمْ
مَّرْجِعُهُمْ فَيُنَبِّئُهُمْ بِمَا كَانُوْا يَعْمَلُوْنَ ﴿١٠٨﴾

109. Wala msiwatukane wale ambao wanawaita kinyume cha Allah wasije wakamtukana Allah kwa uadui bila kujua. Hivyo Tumewapambia kila watu vitendo vyao, kisha marejeo yao yatakuwa kwa Mola wao, naye Atawaambia waliyokuwa wakitenda.

وَاَقْسَمُوْا بِاللّٰهِ جَهْدَ اَيْمَانِهِمْ لَئِنْ
جَآءَتْهُمْ اٰيَةٌ لَّيُؤْمِنُنَّ بِهَا ؕ قُلْ اِنَّمَا

110. Na huapa kwa Allah kwa viapo vyao vyenye nguvu, kama ikiwafikia Ishara kwa yakini wataiamini. Sema: Hakika Ishara ziko

---

Aya 104. *Latiif,* Neno hili maana yake ni (1) mpole, na mwema; (2) asiyeonekana kwa macho; (3) anayejua visivyoonekana. Nalo ni sifa mojawapo ya Allah (Taj, Lisan na Akrab).

Baadhi ya watu wanafikiri ya kuwa wanaweza kumjua Allah kwa uwezo wa fahamu zao. Aya hii inavunja kabisa wazo hili, na inasema ya kuwa ni Allah Mwenyewe Anayeweza kujidhihirisha kwa watu na atie nuru katika fahamu za mtu ndipo aweze kumtambua. Na kwa kutimiza jambo hili Allah Amemwekea mtu njia za kufuata ili aweze kumfikia.

الْاٰيٰتُ عِنْدَ اللّٰهِ وَمَا يُشْعِرُكُمْ ۙ اَنَّهَاۤ اِذَا جَآءَتْ لَا يُؤْمِنُوْنَ ﴿۱۰۹﴾

kwa Allah; na ni kitu gani kitawatambulishieni ya kuwa itakapofika hawataamini.

وَنُقَلِّبُ اَفْـِٕدَتَهُمْ وَاَبْصَارَهُمْ كَمَا لَمْ يُؤْمِنُوْا بِهٖۤ اَوَّلَ مَرَّةٍ وَّنَذَرُهُمْ فِيْ طُغْيَانِهِمْ يَعْمَهُوْنَ ﴿۱۱۰﴾ ع ۱۹

111. Nasi Tutaigeuza mioyo yao na macho yao kwa kuwa hawakuiamini mara ya kwanza na Tutawaacha katika maasi yao wakitangatanga ovyo.

JUZU 8

FUNGU 14

وَلَوْ اَنَّنَا نَزَّلْنَاۤ اِلَيْهِمُ الْمَلٰٓئِكَةَ وَكَلَّمَهُمُ الْمَوْتٰى وَحَشَرْنَا عَلَيْهِمْ كُلَّ شَيْءٍ قُبُلًا مَّا كَانُوْا لِيُؤْمِنُوْۤا اِلَّاۤ اَنْ يَّشَآءَ اللّٰهُ وَلٰكِنَّ اَكْثَرَهُمْ يَجْهَلُوْنَ ﴿۱۱۱﴾

112. Na lau kama Tungewateremshia Malaika, na wafu wakazungumza nao, na Tukawakusanyia kila kitu ana kwa ana, wasingaliamini, isipokuwa Atake Allah; lakini wengi wao wamo ujingani.

وَكَذٰلِكَ جَعَلْنَا لِكُلِّ نَبِيٍّ عَدُوًّا شَيٰطِيْنَ الْاِنْسِ وَالْجِنِّ يُوْحِيْ بَعْضُهُمْ اِلٰى بَعْضٍ زُخْرُفَ الْقَوْلِ غُرُوْرًا ؕ وَلَوْ شَآءَ رَبُّكَ مَا فَعَلُوْهُ فَذَرْهُمْ وَمَا يَفْتَرُوْنَ ﴿۱۱۲﴾

113. Na kama hivyo tukamfanyia kila Nabii adui, mashetani, katika watu na majinni. Baadhi yao wanawafunulia wengine maneno ya ushaufu kuwadanganya, na kama Mola wako Angalipenda wasingalifanya hayo; basi waache na wanayoyatunga.

Aya 112. Ishara hizi zote zilionekana katika wakati wa Mtume s.a.w. Malaika walionekana siku ya vita vya Badri, hata baadhi ya makafiri waliwaona (Jariri jalada 4 uk. 47), lakini wenye mioyo migumu hawakuamini. Walijua sana kuwa Mtume s.a.w. ni mkweli, lakini kwa sababu ya kuzungukwa na watu wabaya na tamaa mbaya wakakataa madai yake.

Aya 113. *Zukhrufal qaul,* "Maneno ya ushaufu." Neno *Zukhruf* maana yake ni dhahabu; pambo lo lote; pia kitu kilichopambwa; kitu kilichopambwa kwa rangi za uwongo au kwa uwongo (Akrab).

Maneno haya: *watu na majinni,* ambayo yanapatikana katika Aya nyingi za Qur'an, hayaonyeshi viumbe vya namna mbili mbalimbali, bali yanaonyesha watu wa namna mbili. *Ins* ni watu wote wa kawaida na *Jinn* ni watu wakubwa wasiochanganyika ovyo na watu wengine, na hawaonekani mara kwa mara. Viongozi waovu wameitwa majinni na wafuasi wao ni watu wajinga. Hao wote huwa ni adui za Mitume.

وَلِتَصْغٰٓى اِلَيْهِ اَفْـِٕدَةُ الَّذِيْنَ لَا يُؤْمِنُوْنَ بِالْاٰخِرَةِ وَلِيَرْضَوْهُ وَلِيَقْتَرِفُوْا مَا هُمْ مُّقْتَرِفُوْنَ ﴿١١٤﴾

114. Na ili ielekee kwayo mioyo ya wale wasioamini Akhera, na ili wayaridhie, na ili wayachume wanayoyachuma.

اَفَغَيْرَ اللّٰهِ اَبْتَغِيْ حَكَمًا وَّهُوَ الَّذِيْٓ اَنْزَلَ اِلَيْكُمُ الْكِتٰبَ مُفَصَّلًا ؕ وَالَّذِيْنَ اٰتَيْنٰهُمُ الْكِتٰبَ يَعْلَمُوْنَ اَنَّهٗ مُنَزَّلٌ مِّنْ رَّبِّكَ بِالْحَقِّ فَلَا تَكُوْنَنَّ مِنَ الْمُمْتَرِيْنَ ﴿١١٥﴾

115. Je, nimfuate hakimu ghairi ya Allah hali Yeye ndiye Amewaterem shieni Kitabu kielezacho waziwazi? Na wale Tuliowapa Kitabu wanajua kwamba hicho kimeteremshwa na Mola wako kwa haki. Basi usiwe miongoni mwa wenye shaka.

وَتَمَّتْ كَلِمَتُ رَبِّكَ صِدْقًا وَّعَدْلًا ؕ لَا مُبَدِّلَ لِكَلِمٰتِهٖ ۚ وَهُوَ السَّمِيْعُ الْعَلِيْمُ ﴿١١٦﴾

116. Na limetimia neno la Mola wako kwa kweli na uadilifu. Hakuna awezaye kuyabadilisha manenoYake, na Yeye ndiye Asikiaye, Ajuaye.

وَاِنْ تُطِعْ اَكْثَرَ مَنْ فِى الْاَرْضِ يُضِلُّوْكَ عَنْ سَبِيْلِ اللّٰهِ ؕ اِنْ يَّتَّبِعُوْنَ اِلَّا الظَّنَّ وَاِنْ هُمْ اِلَّا يَخْرُصُوْنَ ﴿١١٧﴾

117. Na kama ukiwatii wengi wa wale waliomo ardhini watakupoteza katika njia ya Allah. Hawafuati ila dhana, na hawana ila kukisia tu.

اِنَّ رَبَّكَ هُوَ اَعْلَمُ مَنْ يَّضِلُّ عَنْ سَبِيْلِهٖ ۚ وَهُوَ اَعْلَمُ بِالْمُهْتَدِيْنَ ﴿١١٨﴾

118. Bila shaka Mola wako ndiye Anawajua sana walioipotea njia Yake, na Anawajua sana wenye kuongoka.

فَكُلُوْا مِمَّا ذُكِرَ اسْمُ اللّٰهِ عَلَيْهِ اِنْ كُنْتُمْ بِاٰيٰتِهٖ مُؤْمِنِيْنَ ﴿١١٩﴾

119. Basi kuleni katika wale walio somewa jina la Allah ikiwa ninyi mnazi amini Aya Zake.

Maneno ya ushaufu ni hoja wanazoambiana ambazo zinaonekana kana kwamba ni za kweli na imara, lakini kumbe ni za uwongo na ziko wazi, nazo zinatolewa ili kuwadanganya wenye akili ndogo.

Aya 115. Maneno haya, *nimtafute hakimu ghairi ya Allah?* yanaonyesha kuwa katika mambo ya dini Allah tu ndiye anaweza kufanywa hakimu. Vitabu vilivyoandikwa na wanazuoni wa dini haviwezi kutufanya tuache maneno yaliyoteremshwa na Allah, wala hakuna mwanadamu ye yote anayeweza kuwa hakimu katika mambo ya imani. Mungu tu ndiye Hakimu, na neno Lake tu ndilo linaloweza kuongoza katika ukweli.

Aya 116. *Hakuna awezaye kuyabadilisha maneno Yake,* mradi wake ni kuwa bishara anazoeleza Allah kuwa zitatokea, mtu hawezi kuzibadilisha, na kadhalika kanuni Zake hakuna awezaye kuzibadilisha. Ikumbukwe ya kuwa kanuni ya Allah ni ile iliyoelezwa waziwazi katika Qur'an. Mojawapo katika sheria za Mungu zilizoelezwa katika Qur'an ni kwamba Wajumbe Wake wanashinda na maadui zao wanashindwa.

وَمَا لَكُمْ اَلَّا تَاْكُلُوْا مِمَّا ذُكِرَ اسْمُ اللّٰهِ عَلَيْهِ وَقَدْ فَصَّلَ لَكُمْ مَّا حَرَّمَ عَلَيْكُمْ اِلَّا مَا اضْطُرِرْتُمْ اِلَيْهِ ؕ وَاِنَّ كَثِيْرًا لَّيُضِلُّوْنَ بِاَهْوَآئِهِمْ بِغَيْرِ عِلْمٍ ؕ اِنَّ رَبَّكَ هُوَ اَعْلَمُ بِالْمُعْتَدِيْنَ ﴿۱۱۹﴾

120. Na mmekuwaje hamli katika (wanyama) wale waliosomewa jina la Allah na hali Amewabainishieni waziwazi Alivyowaharimishieni, isipokuwa vile mlivyovishurutishwa? Na hakika wengi wanapoteza (wengine) kwa matamanio yao bila elimu. Bila shaka Mola wako ndiye Awajuaye sana warukao mipaka.

وَذَرُوْا ظَاهِرَ الْاِثْمِ وَبَاطِنَهٗ ؕ اِنَّ الَّذِيْنَ يَكْسِبُوْنَ الْاِثْمَ سَيُجْزَوْنَ بِمَا كَانُوْا يَقْتَرِفُوْنَ ﴿۱۲۰﴾

121. Na acheni dhambi iliyo dhahiri na iliyofichika; hakika wale wanaochuma dhambi hivi karibuni watalipwa yale waliyokuwa wakiyachuma.

وَلَا تَاْكُلُوْا مِمَّا لَمْ يُذْكَرِ اسْمُ اللّٰهِ عَلَيْهِ وَاِنَّهٗ لَفِسْقٌ ؕ وَاِنَّ الشَّيٰطِيْنَ لَيُوْحُوْنَ اِلٰٓى اَوْلِيٰٓئِهِمْ لِيُجَادِلُوْكُمْ ۚ وَاِنْ اَطَعْتُمُوْهُمْ اِنَّكُمْ لَمُشْرِكُوْنَ ﴿۱۲۱﴾ ع

122. Wala msile katika wale wasiosomewa jina la Allah, maana huo kwa hakika ni uasi. Na kwa yakini mashetani wanawafunulia marafiki zao kubishana nanyi. Na kama mkiwatii, hakika ninyi mtakuwa washirikina.

FUNGU 15

اَوَمَنْ كَانَ مَيْتًا فَاَحْيَيْنٰهُ وَجَعَلْنَا لَهٗ نُوْرًا يَّمْشِىْ بِهٖ فِى النَّاسِ كَمَنْ مَّثَلُهٗ فِى الظُّلُمٰتِ لَيْسَ بِخَارِجٍ مِّنْهَا ؕ كَذٰلِكَ زُيِّنَ لِلْكٰفِرِيْنَ مَا كَانُوْا يَعْمَلُوْنَ ﴿۱۲۲﴾

123. Je, aliyekuwa mfu kisha Tukamhuisha na Tukamjaalia nuru, ambayo kwayo hutembea katika watu, anaweza kuwa sawa na yule aliyeko gizani asiyeweza kutoka humo? Hivi ndivyo yamepambwa kwa makafiri waliyokuwa wakiyafanya.

Aya 120. *Wanapoteza,* ni neno linaloonyesha ya kwamba mafundisho yanayotengenezwa na watu, ambayo watu wengi huyaleta ili kupinzana na mafundisho ya Allah, ni mafundisho yenye kuwapoteza watu.

Aya 121. Kuna mambo ambayo waziwazi yanaonekana maovu, na mengineyo yanaonekana kuwa mazuri lakini hakika yao ni maovu, au hata kama hayaonekani kuwa mabaya lakini uovu uliomo ndani yao unafichama na hauonekani. Hapa Qur'an inawafunza Waislamu wajiepushe na yote mawili, maana kuwa mtawa kunataka hivyo.

وَكَذٰلِكَ جَعَلْنَا فِيْ كُلِّ قَرْيَةٍ اَكٰبِرَ مُجْرِمِيْهَا لِيَمْكُرُوْا فِيْهَا ؕ وَمَا يَمْكُرُوْنَ اِلَّا بِاَنْفُسِهِمْ وَمَا يَشْعُرُوْنَ ﴿١٢٤﴾

124. Na kadhalika Tukajaalia katika kila mji wakuu wa wakosefu wake ili wafanye humo hila.wala hawazifanyii hil-a isipokuwa nafsi zao,lakini hawatambui.

وَاِذَا جَآءَتْهُمْ اٰيَةٌ قَالُوْا لَنْ نُّؤْمِنَ حَتّٰى نُؤْتٰى مِثْلَ مَآ اُوْتِيَ رُسُلُ اللّٰهِ ؔۘ اَللّٰهُ اَعْلَمُ حَيْثُ يَجْعَلُ رِسَالَتَهٗ ؕ سَيُصِيْبُ الَّذِيْنَ اَجْرَمُوْا صَغَارٌ عِنْدَ اللّٰهِ وَعَذَابٌ شَدِيْدٌ ۢ بِمَا كَانُوْا يَمْكُرُوْنَ ﴿١٢٥﴾

125. Na inapowafikia Ishara, huse-ma: Hatuwezi kuamini mpaka tupewe sawa na yale waliyopewa Mitume wa Mungu. Allah ndiye Ajuaye zaidi Ataka-poweka ujumbe Wake. Hivi karibuni itawafikia waliokosa fedheha kutoka kwa Allah na adhabu kali kwa sababu walikuwa wakifanya hila.

فَمَنْ يُّرِدِ اللّٰهُ اَنْ يَّهْدِيَهٗ يَشْرَحْ صَدْرَهٗ لِلْاِسْلَامِ ۚ وَمَنْ يُّرِدْ اَنْ يُّضِلَّهٗ يَجْعَلْ صَدْرَهٗ ضَيِّقًا حَرَجًا كَاَنَّمَا يَصَّعَّدُ فِي السَّمَآءِ ؕ كَذٰلِكَ يَجْعَلُ اللّٰهُ الرِّجْسَ عَلَى الَّذِيْنَ لَا يُؤْمِنُوْنَ ﴿١٢٦﴾

126. Basi yule ambaye Allah Anataka kumwongoza, Humfungulia kifua chake kwa ajili ya Uislamu; na yule ambaye Anataka kumhukumu apotee, Hukibana kifua chake kana kwamba anapanda mbinguni. Hivi ndivyo Allah Awekavyo adhabu kwa wale wasioamini.

Aya 124. Maneno; *akaabira mujrimiihaa,* kwa tafsiri ya neno kwa neno yana maana ya wale walio wakubwa miongoni mwa wenye dhambi wa mji ule. Neno wakubwa laweza kuwa na maana ya wale wenye hisa kubwa ya dhambi na kwa hiyo basi wanajitokeza miongoni mwao kama viongozi au laweza kuwa na maana ya wanachama wakubwa na wenye ushawishi wa jamii yenye dhambi.

Aya inaeleza ya kuwa wale viongozi waovu waliotajwa katika Aya 113 waliozungukwa na giza kubwa la ujinga (Aya 123), wanazidi katika juhudi yao ya kuzuia maendeleo ya Mitume; na mwishowe wanaangamia wenyewe.

Aya 125. Aya hii inaeleza hoja ya mwisho ya wasioamini katika majadiliano haya. Wanasema, "Hatutaamini wahyi wa Allah mpaka nasi tupate wahyi wa namna hiyo hiyo. Kama Mungu anazungumza nao hao Mitume, basi na azungumze nasi pia." Allah anajibu hoja hii ya upumbavu kwa kusema, "Mungu hazungumzi na kila mtu; anazungumza na yule tu anayemwona kuwa anastahili na anayemchagua." Watu ambao kwa vitendo vyao wanastahiki, kufedheheshwa hawawezi kutukuzwa na Allah. Wao mwisho wao ni kupata fedheha na adhabu kali.

Aya 126. Neno *swadru* laweza kutafsiriwa kama moyo. (Tazama Al-Munjid).
Amtakaye Allah kumwongoza ni mtu Mwenye matendo mema yanayompendeza Allah.

وَهٰذَا صِرَاطُ رَبِّكَ مُسْتَقِيْمًا ؕ قَدْ فَصَّلْنَا الْاٰيٰتِ لِقَوْمٍ يَّذَّكَّرُوْنَ ﴿۱۲۷﴾

127. Na hii ndio njia ya Mola wako iliyonyooka. Bila shaka Tumeeleza Ishara kwa watu wenye kukumbuka.

لَهُمْ دَارُ السَّلٰمِ عِنْدَ رَبِّهِمْ وَهُوَ وَلِيُّهُمْ بِمَا كَانُوْا يَعْمَلُوْنَ ﴿۱۲۸﴾

128. Watapata nyumba ya salama kwa Mola wao, Naye ni Mlinzi wao kwa sababu ya yale waliyokuwa wakiyatenda.

وَيَوْمَ يَحْشُرُهُمْ جَمِيْعًا ۚ يٰمَعْشَرَ الْجِنِّ قَدِ اسْتَكْثَرْتُمْ مِّنَ الْاِنْسِ ۚ وَقَالَ اَوْلِيٰٓؤُهُمْ مِّنَ الْاِنْسِ رَبَّنَا اسْتَمْتَعَ بَعْضُنَا بِبَعْضٍ وَّبَلَغْنَآ اَجَلَنَا الَّذِيْٓ اَجَّلْتَ لَنَا ؕ قَالَ النَّارُ مَثْوٰىكُمْ خٰلِدِيْنَ فِيْهَآ اِلَّا مَا شَآءَ اللّٰهُ ؕ اِنَّ رَبَّكَ حَكِيْمٌ عَلِيْمٌ ﴿۱۲۹﴾

129. Na siku Atakapowakusanya wote, (Atawaambia), Enyi makundi ya majinni! hakika ninyi mmechukua wafuasi wengi katika wanadamu Na marafiki wao katika wanadamu watasema: Mola wetu, tulinufaishana sisi kwa sisi, na tumefikia muda wetu Uliotuwekea. Atasema: Moto ndio makazi yenu, mtakaa humo ila Apende Allah; hakika Mola wako ndiye Mwenye hekima Ajuaye.

وَكَذٰلِكَ نُوَلِّيْ بَعْضَ الظّٰلِمِيْنَ بَعْضًا بِمَا كَانُوْا يَكْسِبُوْنَ ﴿۱۳۰﴾ ع ۱۶

130. Na hivi hivi Tukawatawalisha baadhi ya wadhalimu juu ya wengine kwa sababu ya yale waliyokuwa wakiya chuma.

FUNGU 16

يٰمَعْشَرَ الْجِنِّ وَالْاِنْسِ اَلَمْ يَاْتِكُمْ رُسُلٌ مِّنْكُمْ يَقُصُّوْنَ عَلَيْكُمْ اٰيٰتِيْ وَيُنْذِرُوْنَكُمْ لِقَآءَ يَوْمِكُمْ هٰذَا ؕ قَالُوْا شَهِدْنَا عَلٰٓى اَنْفُسِنَا وَغَرَّتْهُمُ الْحَيٰوةُ الدُّنْيَا وَشَهِدُوْا عَلٰٓى اَنْفُسِهِمْ اَنَّهُمْ كَانُوْا كٰفِرِيْنَ ﴿۱۳۱﴾

131. Enyi makundi ya majinni na wanadamu! Je hawakuwafikieni Mitume toka miongoni mwenu kuwabainishi eni Aya Zangu na kuwaonyeni juu ya mkutano wa siku yenu hii? Watasema: Tumeshuhudia juu ya nafsi zetu. Na yaliwadanganya maisha ya dunia. Nao watajishuhudia wenyewe ya kwamba walikuwa makafiri.

Aya 129. Ni dhahiri katika Aya hii neno *Jinn* (majini) ni *watu wakubwa* ambao wamewapoteza watu wengi wanaowafuata.

Maneno haya, *Moto ndio makazi yenu,* wanaambiwa watu wa kawaida ambao watajitetea kuwa si kosa lao ila ni la wakubwa waliowapoteza. Wanaambiwa sasa kulalama hakutawafaa kitu, lazima waingie Motoni wote, wakubwa na maskini, wenye hatia.

Aya 131. Maneno haya, *Mitume toka miongoni mwenu,* yanazidi kushuhudia kuwa jinni

ذٰلِكَ اَنْ لَّمْ يَكُنْ رَّبُّكَ مُهْلِكَ الْقُرٰى
بِظُلْمٍ وَّ اَهْلُهَا غٰفِلُوْنَ ﴿١٣٢﴾

132. Hayo ni kwa sababu ya kuwa Mola wako Hakuwa wa kuiangamiza miji kwa dhuluma, hali wenyeji wake wameghafilika.

وَ لِكُلٍّ دَرَجٰتٌ مِّمَّا عَمِلُوْا ؕ وَ مَا رَبُّكَ
بِغَافِلٍ عَمَّا يَعْمَلُوْنَ ﴿١٣٣﴾

133. Na wote wana madaraja sawa na yale waliyoyatenda. Na Mola wako si Mwenye kughafilika na yale wanayoyatenda.

وَ رَبُّكَ الْغَنِيُّ ذُو الرَّحْمَةِ ؕ اِنْ يَّشَاْ
يُذْهِبْكُمْ وَ يَسْتَخْلِفْ مِنْۢ بَعْدِكُمْ مَّا يَشَآءُ
كَمَاۤ اَنْشَاَكُمْ مِّنْ ذُرِّيَّةِ قَوْمٍ اٰخَرِيْنَ ﴿١٣٤﴾ؕ

134. Na Mola wako ndiye Mkwasi, Mwenye rehema. Kama Akipenda Atawaondoeni na kuweka wengine Awapendao baada yenu kama vile alivyowaumbeni katika wazao wa watu wengine.

اِنَّ مَا تُوْعَدُوْنَ لَاٰتٍ ۙ وَّ مَاۤ اَنْتُمْ
بِمُعْجِزِيْنَ ﴿١٣٥﴾

135. Kwa yakini mnayoahidiwa yatafika, wala hamtaweza kuepuka.

قُلْ يٰقَوْمِ اعْمَلُوْا عَلٰى مَكَانَتِكُمْ اِنِّيْ
عَامِلٌ ۚ فَسَوْفَ تَعْلَمُوْنَ ۙ مَنْ تَكُوْنُ لَهٗ
عَاقِبَةُ الدَّارِ ؕ اِنَّهٗ لَا يُفْلِحُ الظّٰلِمُوْنَ ﴿١٣٦﴾

136. Sema: Enyi watu wangu tendeni katika makao yenu, mimi pia natenda. Hivi karibuni mtajua ni nani atakuwa na makao (mema) mwishoni. Hakika wadhalimu hawastawi.

وَ جَعَلُوْا لِلّٰهِ مِمَّا ذَرَاَ مِنَ الْحَرْثِ وَ الْاَنْعَامِ
نَصِيْبًا فَقَالُوْا هٰذَا لِلّٰهِ بِزَعْمِهِمْ وَ هٰذَا
لِشُرَكَآئِنَا ۚ فَمَا كَانَ لِشُرَكَآئِهِمْ فَلَا

137. Na wakamfanyia Allah sehemu katika mimea Aliyoiumba na katika wanyama, na husema: Hii ni ya Allah, kwa madai yao, na hii ni ya miungu wetu. Na vilivyokuwa vya miungu wao,

---

si viumbe wa namna nyingine, ni watu hawa hawa. Tunasoma katika Qur'an ya kuwa Mtume Musa na Mtume s.a.w. walipelekwa kuwa Mitume kwa majinni pia (sura 46:30-33; na 72:2-16); nasi hatuoni alama ya Mitume wa kijinni kupelekwa kwa majinni. Jambo hili linaonyesha kuwa neno *Jinn* hapa linahusu watu maalumu. Pia ikumbukwe neno hili linapotumiwa kwa ajili ya watu wakubwa na wenye nguvu huwa linawahusu wale wabaya miongoni mwao.

Aya 132. *Al-Quraa,* "Miji," mradi wake ni miji na vijiji walikopelekwa Manabii wa Allah. Na kwa kuwa Mtume *s.a.w.* alitumwa kwa dunia nzima, kwake neno hili litatumika kwa ajili ya dunia yote.

Aya 136. *I'maluu 'alaa makaanatikum,* "Tendeni katika makao yenu," mradi wake ni fanyeni mwezavyo, au fanyeni vizuri kadiri mwezavyo, au kaeni mlipo na mfanye ubaya wenu wote (Kashshaaf). Makafiri wanaambiwa hapa ya kuwa wafanye kila namna ya juhudi yao kukiangamiza kikundi kidogo cha Waislamu, lakini hawatafanikiwa kamwe.

يَصِلُ اِلَى اللّٰهِ ۚ وَمَا كَانَ لِلّٰهِ فَهُوَ يَصِلُ اِلٰى شُرَكَآئِهِمْ ؕ سَآءَ مَا يَحْكُمُوْنَ ﴿١٣٧﴾

basi havifiki kwa Allah, na vilivyokuwa vya Allah, basi hivyo hufika kwa miungu wao. Ni mabaya wanayoyahukumu.

وَكَذٰلِكَ زَيَّنَ لِكَثِيْرٍ مِّنَ الْمُشْرِكِيْنَ قَتْلَ اَوْلَادِهِمْ شُرَكَآؤُهُمْ لِيُرْدُوْهُمْ وَلِيَلْبِسُوْا عَلَيْهِمْ دِيْنَهُمْ ؕ وَلَوْ شَآءَ اللّٰهُ مَا فَعَلُوْهُ فَذَرْهُمْ وَمَا يَفْتَرُوْنَ ﴿١٣٨﴾

138. Na hivyo washirika wao wamewapambia washirikina wengi kuwaua watoto wao, ili kuwaangamiza na kuwavurugia dini yao. Na kama Allah Angependa wasingalifanya hayo; basi waache na hayo wanayoyatunga.

وَقَالُوْا هٰذِهٖۤ اَنْعَامٌ وَّحَرْثٌ حِجْرٌ ۖ لَّا يَطْعَمُهَاۤ اِلَّا مَنْ نَّشَآءُ بِزَعْمِهِمْ وَاَنْعَامٌ حُرِّمَتْ ظُهُوْرُهَا وَاَنْعَامٌ لَّا يَذْكُرُوْنَ اسْمَ اللّٰهِ عَلَيْهَا افْتِرَآءً عَلَيْهِ ؕ سَيَجْزِيْهِمْ بِمَا كَانُوْا يَفْتَرُوْنَ ﴿١٣٩﴾

139. Nao husema: Wanyama hawa na mimea hii vimekatazwa, hawatavila ila wale tuwapendao, kwa madai yao; na wanyama ambao migongo yao imeharimishwa (kupandwa), na wanyama ambao hawalitaji jina la Allah juu yao - wakimtungia uwongo. Hivi karibuni Atawalipa kwa yale waliyokuwa wakiyatunga.

وَقَالُوْا مَا فِيْ بُطُوْنِ هٰذِهِ الْاَنْعَامِ خَالِصَةٌ لِّذُكُوْرِنَا وَمُحَرَّمٌ عَلٰۤى اَزْوَاجِنَا ۚ وَاِنْ يَّكُنْ مَّيْتَةً فَهُمْ فِيْهِ شُرَكَآءُ ؕ سَيَجْزِيْهِمْ وَصْفَهُمْ ؕ اِنَّهٗ حَكِيْمٌ عَلِيْمٌ ﴿١٤٠﴾

140. Na husema: Waliomo matumboni mwa wanyama hawa hasa ni kwa ajili ya wanaume wetu, na wameharamishwa kwa wake zetu, lakini ikiwa nyamafu, basi wanashirikiana. Hakika Atawalipa maelezo yao. Bila shaka Yeye ni Mwenye hekima, Ajuaye.

قَدْ خَسِرَ الَّذِيْنَ قَتَلُوْۤا اَوْلَادَهُمْ سَفَهًا بِغَيْرِ عِلْمٍ وَّحَرَّمُوْا مَا رَزَقَهُمُ اللّٰهُ افْتِرَآءً عَلَى اللّٰهِ ؕ قَدْ ضَلُّوْا وَمَا كَانُوْا مُهْتَدِيْنَ ﴿١٤١﴾ ع

141. Hakika wamehasirika wale ambao wamewaua watoto wao kwa upumbavu pasipo kujua, na kuharamisha Alivyowaruzuku Allah kwa kumtungia uwongo Allah. Bila shaka wamepotea wala hawakuwa wenye kuongoka.

Aya 139. *Hijr*. Neno hili maana yake ni "iliyokatazwa" au "iliyoharimishwa" ; pia maana yake ni "kipawa cha akili na fahamu", maana kinamzuia mtu asitende matendo yasiyo sawa. Neno hili pia maana yake ni hifadhi au ulinzi (Akrab).
Mimea iliyokatazwa ni ile waliyoitoa wakfu kwa masanamu na iliweza kutumiwa na makuhani tu waliokuwa wakiangalia masanamu. Hata wanyama hawakuruhusiwa kula mimea hiyo. Na wanyama ambao migongo yao iliharimishwa ni hao waliotajwa katika sura 5:104. Na wanyama wasiotajiwa jina la Mungu ni hao waliowatoa wakfu kwa miungu mingine.

FUNGU 17

وَهُوَ الَّذِیۡۤ اَنۡشَاَ جَنّٰتٍ مَّعۡرُوۡشٰتٍ وَّ غَیۡرَ مَعۡرُوۡشٰتٍ وَّ النَّخۡلَ وَالزَّرۡعَ مُخۡتَلِفًا اُكُلُهٗ وَالزَّیۡتُوۡنَ وَالرُّمَّانَ مُتَشَابِهًا وَّغَیۡرَ مُتَشَابِهٍ ؕ كُلُوۡا مِنۡ ثَمَرِهٖۤ اِذَاۤ اَثۡمَرَ وَاٰتُوۡا حَقَّهٗ یَوۡمَ حَصَادِهٖ ۖ وَلَا تُسۡرِفُوۡا ؕ اِنَّهٗ لَا یُحِبُّ الۡمُسۡرِفِیۡنَ ﴿۱۴۱﴾

142. Naye ndiye Aliyeziumba bustani zilizoegemezwa na zisizoegemezwa, na mitende na mimea yenye matunda mbalimbali, na mizaituni na mikomamanga inayofanana na isiyofanana. Kuleni matunda yake ipambapo, na toeni haki yake siku ya kuvunwa kwake, wala msitumie kwa fujo; hakika Yeye hawapendi watumiao kwa fujo.

وَمِنَ الۡاَنۡعَامِ حَمُوۡلَةً وَّ فَرۡشًا ؕ كُلُوۡا مِمَّا رَزَقَكُمُ اللّٰهُ وَلَا تَتَّبِعُوۡا خُطُوٰتِ الشَّیۡطٰنِ ؕ اِنَّهٗ لَكُمۡ عَدُوٌّ مُّبِیۡنٌ ﴿۱۴۲﴾

143. Na wako katika wanyama wabebao mizigo na watambaao. Kuleni katika vile Alivyokuruzukuni Allah, wala msifuate nyayo za Shetani; kwa yakini yeye ni adui yenu dhahiri.

ثَمٰنِیَةَ اَزۡوَاجٍ ۚ مِنَ الضَّاۡنِ اثۡنَیۡنِ وَمِنَ الۡمَعۡزِ اثۡنَیۡنِ ؕ قُلۡ ءٰٓالذَّكَرَیۡنِ حَرَّمَ اَمِ الۡاُنۡثَیَیۡنِ اَمَّا اشۡتَمَلَتۡ عَلَیۡهِ اَرۡحَامُ الۡاُنۡثَیَیۡنِ ؕ نَبِّـُٔوۡنِیۡ بِعِلۡمٍ اِنۡ كُنۡتُمۡ صٰدِقِیۡنَ ﴿۱۴۳﴾

144. Ameumba wenzi wanane wakiwamo wawili wa kondoo na wawili wa mbuzi. Sema: Je, Ameharamisha madume wawili au majike wawili, au waliomo matumboni mwa majike wawili? Niambieni kwa elimu ikiwa ninyi mnasema kweli.

وَمِنَ الۡاِبِلِ اثۡنَیۡنِ وَمِنَ الۡبَقَرِ اثۡنَیۡنِ ؕ قُلۡ ءٰٓالذَّكَرَیۡنِ حَرَّمَ اَمِ الۡاُنۡثَیَیۡنِ اَمَّا اشۡتَمَلَتۡ عَلَیۡهِ اَرۡحَامُ الۡاُنۡثَیَیۡنِ ؕ اَمۡ كُنۡتُمۡ شُهَدَآءَ اِذۡ وَصّٰىكُمُ اللّٰهُ بِهٰذَا ۚ فَمَنۡ اَظۡلَمُ مِمَّنِ افۡتَرٰی عَلَی اللّٰهِ كَذِبًا لِّیُضِلَّ النَّاسَ بِغَیۡرِ عِلۡمٍ ؕ اِنَّ اللّٰهَ لَا یَهۡدِی الۡقَوۡمَ الظّٰلِمِیۡنَ ﴿۱۴۴﴾ ع ۱۷

145. Na wawili katika ngamia na wawili katika ng'ombe. Sema: Je Ameharamisha madume wawili au majike wawili, au waliomo matumboni mwa majike wawili? Au, je, ninyi mlikuweko Allah Alipowausieni haya? Basi ni nani mdhalimu mkubwa kuliko yule aliyemtungia Allah uwongo ili kuwapoteza watu bila elimu? Hakika Allah Hawaongozi watu wadhalimu.

Aya 142. Katika Aya zilizopita Qur'an imetaja sheria zilizowekwa na Waarabu wasio na dini, wasiosaidiwa na neno la Mungu. Sasa Qur'an inaeleza baadhi ya sheria zake ili msomaji aweze kuzilinganisha na sheria zilizotengenezwa na watu zilizotajwa hapo juu.

FUNGU 18

قُلْ لَّآ اَجِدُ فِيْ مَآ اُوْحِيَ اِلَيَّ مُحَرَّمًا عَلٰى طَاعِمٍ يَّطْعَمُهٗٓ اِلَّآ اَنْ يَّكُوْنَ مَيْتَةً اَوْ دَمًا مَّسْفُوْحًا اَوْ لَحْمَ خِنْزِيْرٍ فَاِنَّهٗ رِجْسٌ اَوْ فِسْقًا اُهِلَّ لِغَيْرِ اللّٰهِ بِهٖ ۚ فَمَنِ اضْطُرَّ غَيْرَ بَاغٍ وَّلَا عَادٍ فَاِنَّ رَبَّكَ غَفُوْرٌ رَّحِيْمٌ ﴿١٤٦﴾

146. Sema: Sioni katika yale niliyofunuliwa mimi kitu kilichoharamishwa kwa mlaji kukila isipokuwa kiwe ni mzoga au damu iliyomwagika, au nyama ya nguruwe - kwani hivyo ni uchafu; au ni uasi kilichochinjwa kwa jina la asiyekuwa Allah. Lakini aliyeshurutishwa pasipo kupenda wala kuruka mipaka, basi kwa hakika Mola wako ni Mwenye kusamehe, Mwenye rehema.

وَعَلَى الَّذِيْنَ هَادُوْا حَرَّمْنَا كُلَّ ذِيْ ظُفُرٍ ۚ وَمِنَ الْبَقَرِ وَالْغَنَمِ حَرَّمْنَا عَلَيْهِمْ شُحُوْمَهُمَآ اِلَّا مَا حَمَلَتْ ظُهُوْرُهُمَآ اَوِ الْحَوَايَآ اَوْ مَا اخْتَلَطَ بِعَظْمٍ ۭ ذٰلِكَ جَزَيْنٰهُمْ بِبَغْيِهِمْ ۡ وَاِنَّا لَصٰدِقُوْنَ ﴿١٤٧﴾

147. Na kwa wale walio Mayahudi Tuliharimisha kila chenye kucha, na katika ng'ombe na kondoo Tukawaharamishia mafuta yao isipokuwa yale iliyobeba migongo yao au (iliyobeba) matumbo (yao), au yale yaliyogandamana na mifupa. Hayo tuliwalipa kwa sababu ya uasi wao; na bila shaka Sisi ndio Wakweli.

فَاِنْ كَذَّبُوْكَ فَقُلْ رَّبُّكُمْ ذُوْ رَحْمَةٍ وَّاسِعَةٍ ۚ وَلَا يُرَدُّ بَاْسُهٗ عَنِ الْقَوْمِ الْمُجْرِمِيْنَ ﴿١٤٨﴾

148. Lakini wakikukadhibisha, basi sema, Mola wenu ni Mwenye rehema nyingi; na adhabu yake haiondolewi kwa watu wakosefu.

سَيَقُوْلُ الَّذِيْنَ اَشْرَكُوْا لَوْ شَاۗءَ اللّٰهُ مَآ اَشْرَكْنَا وَلَآ اٰبَاۗؤُنَا وَلَا حَرَّمْنَا مِنْ

149. Hivi karibuni wanaoshirikisha watasema: Angalipenda Allah tusingalimshirikisha sisi wala

---

Aya 146. Aya hii inaeleza ya kuwa sheria iliyowekwa na Waarabu wasio na dini juu ya vyakula halali na haramu haikuwa na hekima yo yote; lakini sheria iliyowekwa na dini ya Kiislamu ilikuwa na akili na busara kubwa. Islam inakataza vyakula vya namna nne. Namna tatu vilivyo *rijs,* yaani vichafu, navyo ni (1) mzoga, (2) damu inayomiminika mnyama anapochinjwa au kujeruhiwa, (3) nyama ya nguruwe. Namna ya (4) ni *fisq,* yaani cha ukufuru kisicho cha dini ambacho kinaleta kumwasi Allah. Kula kitu cha namna hiyo kutaua huba na wivu alio nao mtu kwa ajili ya Allah. Pia tazama sura 2:174.

Hapa neno *izturra* linamaanisha kulazimishwa na njaa na kutaabishwa kwa njaa zaidi ya uwezo wa mtu wa kustahmili shinikizo hilo.

شَيْءٍ ؕ كَذٰلِكَ كَذَّبَ الَّذِيْنَ مِنْ قَبْلِهِمْ
حَتّٰى ذَاقُوْا بَاْسَنَا ؕ قُلْ هَلْ عِنْدَكُمْ مِّنْ
عِلْمٍ فَتُخْرِجُوْهُ لَنَا ؕ اِنْ تَتَّبِعُوْنَ اِلَّا
الظَّنَّ وَ اِنْ اَنْتُمْ اِلَّا تَخْرُصُوْنَ ﴿۱۴۹﴾

baba zetu, wala tusingaliharimisha cho chote. Vivi hivi walikadhibisha waliokuwa kabla yao mpaka wakaonja adhabu Yetu. Sema: Je, ninyi mnayo elimu? Basi mtutolee hiyo. Ninyi hamfuati ila dhana tu, wala hamsemi ila uwongo tu.

قُلْ فَلِلّٰهِ الْحُجَّةُ الْبَالِغَةُ ۚ فَلَوْ شَآءَ
لَهَدٰىكُمْ اَجْمَعِيْنَ ﴿۱۵۰﴾

150. Sema: Basi Allah ndiye Mwenye hoja iliyokamilika; na kama Angali penda Angewaongozeni ninyi nyote.

قُلْ هَلُمَّ شُهَدَآءَكُمُ الَّذِيْنَ يَشْهَدُوْنَ اَنَّ
اللّٰهَ حَرَّمَ هٰذَا ۚ فَاِنْ شَهِدُوْا فَلَا تَشْهَدْ
مَعَهُمْ ۚ وَلَا تَتَّبِعْ اَهْوَآءَ الَّذِيْنَ كَذَّبُوْا
بِاٰيٰتِنَا وَالَّذِيْنَ لَا يُؤْمِنُوْنَ بِالْاٰخِرَةِ
وَهُمْ بِرَبِّهِمْ يَعْدِلُوْنَ ﴿۱۵۱﴾ ع

151. Sema: Leteni mashahidi wenu wanaoweza kushuhudia kuwa Allah Amewaharamishia (vitu) hivi.
Basi watoapo ushahidi, wewe usishuhudie pamoja nao, wala usifuate matamanio ya wale waliokadhibisha Aya Zetu na wasioamini Akhera, nao huwashirikisha wengine na Mola wao.

FUNGU 19

قُلْ تَعَالَوْا اَتْلُ مَا حَرَّمَ رَبُّكُمْ عَلَيْكُمْ
اَلَّا تُشْرِكُوْا بِهٖ شَيْـًٔا وَّبِالْوَالِدَيْنِ اِحْسَانًا ۚ
وَلَا تَقْتُلُوْٓا اَوْلَادَكُمْ مِّنْ اِمْلَاقٍ ؕ
نَحْنُ نَرْزُقُكُمْ وَاِيَّاهُمْ ۚ وَلَا تَقْرَبُوا
الْفَوَاحِشَ مَا ظَهَرَ مِنْهَا وَمَا بَطَنَ ۚ وَلَا
تَقْتُلُوا النَّفْسَ الَّتِيْ حَرَّمَ اللّٰهُ اِلَّا بِالْحَقِّ ؕ
ذٰلِكُمْ وَصّٰىكُمْ بِهٖ لَعَلَّكُمْ تَعْقِلُوْنَ ﴿۱۵۲﴾

152. Sema: Njooni niwasomeeni Aliyowaharamishieni Mola wenu: ya kwamba msimshirikishe na chochote, na fanyeni wema kwa wazazi wenu, wala msiwauwe watoto wenu kwa kuhofia umaskini, Sisi Tunawapeni ninyi riziki na wao pia,wala msiyakaribie mambo maovu, yaliyo dhahiri na yaliyo siri; wala msimwue mtu ambaye Allah Ameharamisha (kuuawa) ila kwa haki. Hayo Amewausieni ili mpate kufahamu.

وَلَا تَقْرَبُوْا مَالَ الْيَتِيْمِ اِلَّا بِالَّتِيْ هِيَ
اَحْسَنُ حَتّٰى يَبْلُغَ اَشُدَّهٗ ۚ وَاَوْفُوا الْكَيْلَ
وَالْمِيْزَانَ بِالْقِسْطِ ۚ لَا نُكَلِّفُ نَفْسًا اِلَّا
وُسْعَهَا ۚ وَاِذَا قُلْتُمْ فَاعْدِلُوْا وَلَوْ كَانَ ذَا
قُرْبٰى ۚ وَبِعَهْدِ اللّٰهِ اَوْفُوْا ؕ ذٰلِكُمْ وَصّٰىكُمْ
بِهٖ لَعَلَّكُمْ تَذَكَّرُوْنَ ۙ﴿۱۵۲﴾

153. Wala msikaribie mali ya yatima, isipokuwa kwa njia bora, mpaka afikie baleghe yake. Na kamilisheni kipimo na mizani kwa uadilifu. Hatumkalifishi mtu ila kwa wasaa wake. Na msemapo basi shikeni uadilifu hata kama awe ni jamaa, na tekelezeni ahadi ya Allah. Hayo Amewausieni ili mpate kukumbuka.

وَاَنَّ هٰذَا صِرَاطِيْ مُسْتَقِيْمًا فَاتَّبِعُوْهُ ۚ وَلَا
تَتَّبِعُوا السُّبُلَ فَتَفَرَّقَ بِكُمْ عَنْ سَبِيْلِهٖ ؕ
ذٰلِكُمْ وَصّٰىكُمْ بِهٖ لَعَلَّكُمْ تَتَّقُوْنَ ﴿۱۵۳﴾

154. Na kwa hakika hii ndio njia yangu iliyonyooka, basi ifuateni, wala msifuate njia mbalimbali zikawatengeni mbali na njia Yake. Hayo Amewausieni ili mpate kujilinda.

ثُمَّ اٰتَيْنَا مُوْسَى الْكِتٰبَ تَمَامًا عَلَى الَّذِيْٓ
اَحْسَنَ وَتَفْصِيْلًا لِّكُلِّ شَيْءٍ وَّهُدًى
وَّرَحْمَةً لَّعَلَّهُمْ بِلِقَآءِ رَبِّهِمْ يُؤْمِنُوْنَ ﴿۱۵۴﴾ ع

155. Tena Tulimpa Musa kitabu kwa kutimiza (neema) juu ya yule aliyefanya wema na ni maelezo ya kila kitu na mwongozo na rehema ili wapate kuamini kukutana kwao na Mola wao.

FUNGU 20

وَهٰذَا كِتٰبٌ اَنْزَلْنٰهُ مُبٰرَكٌ فَاتَّبِعُوْهُ
وَاتَّقُوْا لَعَلَّكُمْ تُرْحَمُوْنَ ۙ﴿۱۵۵﴾

156. Na hiki ni Kitabu Tulichokiteremsha, kilichobarikiwa, basi kifuateni na ogopeni ili mrehemiwe.

Aya 155. *Yule aliyefanya wema,* yaani Nabii Musa au mtu ye yote mwenye kufanya wema. Aya hii inaonyesha mambo manne yaliyo ni sababu za kuteremshwa Kitabu: (1) Allah Anataka kutimiza neema zake kwa Kitabu hicho. (2) Kuwa kimekusanya amri zote zinazohitajiwa katika wakati huo. (3) Kinakuwa na njia za kuwaongoza watu kwenye njia iliyo sawa. (4) Kinakuwa ni rehema, yaani wanaokifuata wanapokea baraka kutoka kwa Allah.

Aya 156. *Hiki ni Kitabu,* yaani Qur'an. Kabla ya kutolewa amri ya kufuata Qur'an zimetolewa sababu. Sababu ya kwanza ni kuwa Kitabu hiki kimeteremshwa na Allah. Sababu ya pili, Kitabu hiki ni *mubaarak* (kilichojaa baraka), chenye kila fundisho zuri la vitabu vilivyotangulia.

اَنْ تَقُوْلُوْٓا اِنَّمَآ اُنْزِلَ الْكِتٰبُ عَلٰى
طَآئِفَتَيْنِ مِنْ قَبْلِنَا ۪ وَاِنْ كُنَّا عَنْ
دِرَاسَتِهِمْ لَغٰفِلِيْنَ ۙ﴿۱۵۷﴾

157. Msije mkasema: Hakika Kitabu kiliteremshwa juu ya makundi mawili kabla yetu, nasi tulikuwa hatuna habari ya yale waliyoyasoma.

اَوْ تَقُوْلُوْا لَوْ اَنَّآ اُنْزِلَ عَلَيْنَا الْكِتٰبُ
لَكُنَّآ اَهْدٰى مِنْهُمْ ۚ فَقَدْ جَآءَكُمْ
بَيِّنَةٌ مِّنْ رَّبِّكُمْ وَهُدًى وَّرَحْمَةٌ ۚ فَمَنْ
اَظْلَمُ مِمَّنْ كَذَّبَ بِاٰيٰتِ اللّٰهِ وَصَدَفَ
عَنْهَا ؕ سَنَجْزِي الَّذِيْنَ يَصْدِفُوْنَ عَنْ
اٰيٰتِنَا سُوْٓءَ الْعَذَابِ بِمَا كَانُوْا يَصْدِفُوْنَ ﴿۱۵۸﴾

158. Au mkasema: Lau tungaliteremshiwa Kitabu bila shaka tungalikuwa waongofu zaidi kuliko wao. Basi imewafikieni Ishara iliyo wazi kutoka kwa Mola wenu, na mwongozo na rehema pia. Basi ni nani mdhalimu mkubwa kuliko yule anayezikadhibisha Aya za Allah na kujitenga nazo? Hivi karibuni Tutawalipa wale wanaojitenga na Aya Zetu adhabu mbaya kwa sababu walikuwa wamejitenga.

هَلْ يَنْظُرُوْنَ اِلَّآ اَنْ تَاْتِيَهُمُ الْمَلٰٓئِكَةُ اَوْ
يَاْتِيَ رَبُّكَ اَوْ يَاْتِيَ بَعْضُ اٰيٰتِ رَبِّكَ ؕ يَوْمَ
يَاْتِيْ بَعْضُ اٰيٰتِ رَبِّكَ لَا يَنْفَعُ نَفْسًا
اِيْمَانُهَا لَمْ تَكُنْ اٰمَنَتْ مِنْ قَبْلُ اَوْ
كَسَبَتْ فِيْٓ اِيْمَانِهَا خَيْرًا ؕ قُلِ انْتَظِرُوْٓا
اِنَّا مُنْتَظِرُوْنَ ﴿۱۵۹﴾

159. Hawangoji ila wawafikie Malaika, au Mola wako Afike, au zifike baadhi ya Ishara za Mola wako. Siku zitakapofika baadhi ya Ishara za Mola wako, basi mtu haitamfaa imani yake ambaye hakuamini zamani, au kuchuma heri kwa imani yake. Sema: Ngojeni, sisi pia tunangoja.

اِنَّ الَّذِيْنَ فَرَّقُوْا دِيْنَهُمْ وَكَانُوْا شِيَعًا
لَّسْتَ مِنْهُمْ فِيْ شَيْءٍ ؕ اِنَّمَآ اَمْرُهُمْ اِلَى
اللّٰهِ ثُمَّ يُنَبِّئُهُمْ بِمَا كَانُوْا يَفْعَلُوْنَ ﴿۱۶۰﴾

160. Hakika wale waliofarikisha dini yao na wakawa makundi-makundi, huna uhusiano nao wo wote. Bila shaka shauri lao ni kwa Allah; kisha Atawaambia yale waliyokuwa wakitenda.

Aya 157. *Makundi mawili* ni (1) Mayahudi waliopewa Kitabu cha Musa na ambao dini yao ilianzia upande wa kaskazini ya nchi ya Bara Arabu; na (2) wafuasi wa Zartashti (Zoroaster) waliopewa Kitabu kinachoitwa Zend-Avesta na ambao waliishi upande wa mashariki ya Bara Arabu. Wakristo hawakupewa Sheria ya peke yao, maana Yesu na wanafunzi wake walifuata Sheria ya Musa; hivyo kwa mujibu wa Sheria za dini, Wakristo lazima wawekwe pamoja na Mayahudi.

Aya 159. *Wawafikie Malaika,* mradi wake ni kufika adhabu katika sura ya vita, kwani katika Qur'an kufika kwa Malaika kumetajwa kwa kuhusiana na vita zilizopiganwa baina ya Waislamu na maadui zao.

مَنْ جَآءَ بِالْحَسَنَةِ فَلَهٗ عَشْرُ اَمْثَالِهَا ۚ وَمَنْ جَآءَ بِالسَّيِّئَةِ فَلَا يُجْزٰٓى اِلَّا مِثْلَهَا وَهُمْ لَا يُظْلَمُوْنَ ﴿١٦٠﴾

161. Ajaye na kitendo kizuri, basi atalipwa mfano wake mara kumi zaidi; na ajaye na kitendo kibaya, basi hatalipwa ila sawa nacho; nao hawatadhulumiwa.

قُلْ اِنَّنِيْ هَدٰىنِيْ رَبِّيْٓ اِلٰى صِرَاطٍ مُّسْتَقِيْمٍ ۚ دِيْنًا قِيَمًا مِّلَّةَ اِبْرٰهِيْمَ حَنِيْفًا ۚ وَمَا كَانَ مِنَ الْمُشْرِكِيْنَ ﴿١٦١﴾

162. Sema: Kwa hakika mimi Mola wangu Ameniongoza kwenye njia iliyonyooka kwenye dini iliyo sawa kabisa ndio mila ya Ibrahimu aliye mnyofu na hakuwa miongoni mwa wenye kumshirikisha Allah.

قُلْ اِنَّ صَلَاتِيْ وَنُسُكِيْ وَمَحْيَايَ وَمَمَاتِيْ لِلّٰهِ رَبِّ الْعٰلَمِيْنَ ﴿١٦٢﴾

163. Sema: Hakika Sala yangu, na sadaka yangu, na uzima wangu, na kufa kwangu ni kwa ajili ya Allah, Mola wa walimwengu.

لَا شَرِيْكَ لَهٗ ۚ وَبِذٰلِكَ اُمِرْتُ وَاَنَا اَوَّلُ الْمُسْلِمِيْنَ ﴿١٦٣﴾

164. Hana mshirika. Na hayo ndio niliyoamrishwa, na mimi ni wa kwanza wa waliojisalimisha.

قُلْ اَغَيْرَ اللّٰهِ اَبْغِيْ رَبًّا وَّهُوَ رَبُّ كُلِّ شَيْءٍ ؕ وَلَا تَكْسِبُ كُلُّ نَفْسٍ اِلَّا عَلَيْهَا ۚ وَلَا تَزِرُ وَازِرَةٌ وِّزْرَ اُخْرٰى ۚ ثُمَّ اِلٰى رَبِّكُمْ مَّرْجِعُكُمْ فَيُنَبِّئُكُمْ بِمَا كُنْتُمْ فِيْهِ تَخْتَلِفُوْنَ ﴿١٦٤﴾

165. Sema: Je! nishike mola ghairi ya Allah na hali Yeye ndiye Mola wa kila kitu? Wala nafsi yo yote haichumi ubaya ila inabeba mzigo wake yenyewe. Na wala mbebaji hatabeba mzigo wa mwingine. Kisha marudio ni kwa Mola wenu., naye Atawaambieni yale mliyokuwa mkihitilafiana.

وَهُوَ الَّذِيْ جَعَلَكُمْ خَلٰٓئِفَ الْاَرْضِ وَرَفَعَ بَعْضَكُمْ فَوْقَ بَعْضٍ دَرَجٰتٍ لِّيَبْلُوَكُمْ فِيْ مَآ اٰتٰىكُمْ ؕ اِنَّ رَبَّكَ سَرِيْعُ الْعِقَابِ ۖ وَاِنَّهٗ لَغَفُوْرٌ رَّحِيْمٌ ﴿١٦٥﴾ ع

166. Naye ndiye Aliyewafanyeni warithi katika ardhi na kuwanyanyueni baadhi yenu juu ya wengine katika madaraja, kwa kuwajaribuni kwa hayo Aliyowapeni. Hakika Mola wako ni Mwepesi wa kuadhibu, na hakika Yeye ni Msamehevu sana, Mrehemevu.

Aya 161. Aya hii kwa namna nzuri sana inaeleza jinsi huruma ya Allah inavyotawala hasira na adhabu Yake. Tendo jema linafananishwa na mbegu nzuri inayotoa mazao mara kumi au zaidi (sura 2:262; 4:41; na 10:27-28; pia Tirmidhi sura ya *Saum*), lakini tendo ovu linahesabiwa kuwa moja tu. Aya hii inaonyesha kuwa penye thawabu na adhabu lazima pawe na kanuni.

Aya 163. *Nusuk,* "sadaka" maana yake ni dhabihu, ibada, haki iliyo ni ya Allah, damu ya mnyama anayechinjwa kwa sadaka (Akrab).

Juu ya Sala, Mtume *s.a.w.* alisema, "Burudisho la macho yangu limo ndani ya sala" (Nisai).

سُوْرَةُ الْاَعْرَافِ مَكِّيَّةٌ وَّ هِيَ مَعَ الْبَسْمَلَةِ مِائَتَانِ وَ سَبْعُ اٰيَاتٍ وَّ اَرْبَعَةٌ وَّ عِشْرُوْنَ رُكُوْعًا

7. SURA AL-A'RAAF

Imeteremshwa Makka

Ina mafungu 24 na Aya 207 pamoja na Bismillahi

بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ ①

الٓمّٓصٓ ②

كِتٰبٌ اُنْزِلَ اِلَيْكَ فَلَا يَكُنْ فِيْ صَدْرِكَ حَرَجٌ مِّنْهُ لِتُنْذِرَ بِهٖ وَ ذِكْرٰى لِلْمُؤْمِنِيْنَ ③

اِتَّبِعُوْا مَآ اُنْزِلَ اِلَيْكُمْ مِّنْ رَّبِّكُمْ وَلَا تَتَّبِعُوْا مِنْ دُوْنِهٖٓ اَوْلِيَآءَ ؕ قَلِيْلًا مَّا تَذَكَّرُوْنَ ④

وَكَمْ مِّنْ قَرْيَةٍ اَهْلَكْنٰهَا فَجَآءَهَا بَاْسُنَا بَيَاتًا اَوْ هُمْ قَآئِلُوْنَ ⑤

1. Kwa jina la Allah, Mwingi wa rehema, Mwingi wa ukarimu.
2. Mimi ndiye Allah Nijuaye sana, Mkweli.
3. Kitabu kimeteremshwa kwako, basi kwacho isiwe dhiki kifuani mwako, upate kuonya kwacho, na ni mawaidha kwa waaminio.
4. Fuateni mliyoteremshiwa kutoka kwa Mola wenu, wala msifuate walinzi wengine badala Yake. Ni machache mnayoyakumbuka.
5. Na vijiji vingapi tuliviangamiza! na ilivifikia adhabu Yetu usiku au adhuhuri walipokuwa wamelala.

Ibni Abbas, Ibni Zubair, Hassan, Mujahid, Ikrima, Ata na Jabir bin Zaid wanakubali ya kuwa sura hii ni ya Makka isipokuwa Aya 165 - 172. Katada anasema ya kwamba Aya 165 ilishuka Madina. Neno *A'raaf* maana yake ni "Mwahali mlimwoinuka."

Aya 2. Ibni Abbas anaeleza ya kuwa hizi herufi nne *Alif laam Miim Saad* ni kifupisho cha *Anallahu a'lamu wa afswilu* (Mimi ndiye Mungu,Nijuaye, Nielezaye).Habari zilizomo katika sura hii zinakubali tafsiri hii, maana sura hii si kama ina elimu ya kiungu tu bali pia "inaeleza" sana, na kwa mifano mingi, habari zilizosemwa katika sura iliyotangulia.

Aya 3. Aya hii ni maneno anayoambiwa kila mwaminio wala si Mtume peke yake. Waaminio wanaambiwa, hii Qur'an ni maneno hasa ya Allah Mwenyewe wala si utungaji wa Mtume *s.a.w.* ; na maadamu ni maneno ya Allah Mjuzi wa yote, basi wasisite au kuona dhiki kufuata mafundisho yake na kuwahubiria watu wengine wayafuate.

Aya 4. Hakuna ulinzi wala msaada wa ye yote unaoweza kuwafaa watu wanaoleta upinzani kwa Allah na Mitume Wake. Hili ni somo lililoandikwa bayana katika kurasa za historia na linastahili kukumbukwa.

فَمَا كَانَ دَعْوٰىهُمْ اِذْ جَآءَهُمْ بَاْسُنَآ اِلَّآ اَنْ قَالُوْٓا اِنَّا كُنَّا ظٰلِمِيْنَ ۝٦

6. Basi haikuwa kilio chao ilipowafikia adhabu Yetu isipokuwa walisema: Bila shaka sisi tulikuwa wadhalimu.

فَلَنَسْـَٔلَنَّ الَّذِيْنَ اُرْسِلَ اِلَيْهِمْ وَلَنَسْـَٔلَنَّ الْمُرْسَلِيْنَ ۝٧

7. Na kwa yakini Tutawauliza wale waliopelekewa (Mitume), na pia kwa yakini Tutawauliza (Mitume) waliotumwa.

فَلَنَقُصَّنَّ عَلَيْهِمْ بِعِلْمٍ وَّمَا كُنَّا غَآئِبِيْنَ ۝٨

8. Tena kwa hakika Tutawaambia kwa elimu, wala Hatukuwa mbali.

وَالْوَزْنُ يَوْمَئِذِ ِۨالْحَقُّ ۚ فَمَنْ ثَقُلَتْ مَوَازِيْنُهٗ فَاُولٰٓئِكَ هُمُ الْمُفْلِحُوْنَ ۝٩

9. Na Siku hiyo kipimo kitakuwa sawa. Basi atakayekuwa na uzani mzito, basi hao ndio watakaofaulu.

وَمَنْ خَفَّتْ مَوَازِيْنُهٗ فَاُولٰٓئِكَ الَّذِيْنَ خَسِرُوْٓا اَنْفُسَهُمْ بِمَا كَانُوْا بِاٰيٰتِنَا يَظْلِمُوْنَ ۝١٠

10. Na watakaokuwa na uzani hafifu, basi hao ndio waliohasiri nafsi zao kwa sababu walikuwa wakifanyia jeuri Aya Zetu.

وَلَقَدْ مَكَّنّٰكُمْ فِى الْاَرْضِ وَجَعَلْنَا لَكُمْ فِيْهَا مَعَايِشَ ؕ قَلِيْلًا مَّا تَشْكُرُوْنَ ۝١١ ع

11. Na bila shaka Tumewakalisheni katika ardhi na Tumewawekeeni humo vitu vya maisha. Ni shukurani ndogo tu mnazotoa.

FUNGU 2

وَلَقَدْ خَلَقْنٰكُمْ ثُمَّ صَوَّرْنٰكُمْ ثُمَّ قُلْنَا لِلْمَلٰٓئِكَةِ اسْجُدُوْا لِاٰدَمَ ۖ فَسَجَدُوْٓا اِلَّآ اِبْلِيْسَ ؕ لَمْ يَكُنْ مِّنَ السّٰجِدِيْنَ ۝١٢

12. Na hakika Tuliwaumbeni, kisha Tukawafanyeni sura, kisha Tukawaambia Malaika: Mtiini Adamu. Basi wakatii isipokuwa Ibilisi; hakuwa miongoni mwa wenye kutii.

Aya 12. Sehemu ya habari za Adamu imeelezwa katika sura 2:31-40. Sehemu nyingine ya habari hiyo inaelezwa hapa kwa maelezo zaidi.

Jambo linalofaa kukumbukwa ni kwamba sura 2:31 inatueleza kuwa Adamu aliumbwa hapa hapa ardhini na ya kwamba hakuwa mtu wa kwanza hapa duniani na tena kuliishi watu wengine kabla yeye hajakuwako. Aya hii pia inadhihirisha jambo hilo hilo. Inawaambia watu hivi, *Na hakika Tuliwaumbeni, kisha Tukawafanyeni sura, kisha Tukawaambia Malaika: Mtiini Adamu.* Maneno *Tuliwaumbeni* yamekuja kwanza, na baada yake imesemwa *kisha* Malaika wakaambiwa kumtii Adamu. Maneno haya yanaonyesha kwamba Malaika waliamrishwa kutii baada ya kuumbwa watu, si baada ya kuumbwa Adamu peke yake.

Adamu aliumbwa hapa hapa duniani. Mtume *s.a.w.* akieleza juu ya mahali alipokaa Adamu, alisema ya kwamba Mto Nil (Nile) na mto Furata (Euphrates) ni mito miwili ya *jannat* (bustani)

قَالَ مَا مَنَعَكَ اَلَّا تَسْجُدَ اِذْ اَمَرْتُكَ ؕ قَالَ اَنَا خَيْرٌ مِّنْهُ ۚ خَلَقْتَنِيْ مِنْ نَّارٍ وَّ خَلَقْتَهٗ مِنْ طِيْنٍ ﴿۱۲﴾

13. (Allah) Akasema: Nini kimekuzuia kutii Nilipokuamuru? Akasema: Mimi ni bora kuliko yeye, Umeniumba kwa moto naye Umemwumba kwa udongo.

قَالَ فَاهْبِطْ مِنْهَا فَمَا يَكُوْنُ لَكَ اَنْ تَتَكَبَّرَ فِيْهَا فَاخْرُجْ اِنَّكَ مِنَ الصّٰغِرِيْنَ ﴿۱۳﴾

14. Akasema: Basi ondoka humo, haikufai kufanya kiburi humo! Haya toka; hakika wewe u miongoni mwa wadhalilifu.

قَالَ اَنْظِرْنِيْۤ اِلٰى يَوْمِ يُبْعَثُوْنَ ﴿۱۴﴾

15. Akasema unipe muda mpaka siku watakapofufuliwa.

قَالَ اِنَّكَ مِنَ الْمُنْظَرِيْنَ ﴿۱۵﴾

16. Akasema: Bila shaka u miongoni mwa waliopewa muda.

قَالَ فَبِمَاۤ اَغْوَيْتَنِيْ لَاَقْعُدَنَّ لَهُمْ صِرَاطَكَ الْمُسْتَقِيْمَ ۙ﴿۱۶﴾

17. Akasema: Kwa sababu Umenihukumu mpotevu kwa yakini nitawakalia katika njia yako iliyonyooka.

(Muslim, sura *Jannat*). Hadithi pia inaeleza kuwa Iraq Arab (Mesopotamia) ambayo ni ardhi yenye mito Furata na Tigris, ndipo mahali zilipopatikana habari za Adamu.

Mambo yale ambayo hayathibitiki kwamba yalifanyika hapo kwa kuhusiana na Adamu yaliyoelezwa na Qur'an, hakika yao ni kwamba yameelezwa kwa sura ya mfano na kwa methali. Jambo hili linadhihirika katika habari kama hizi zifuatazo:-

(1) Malaika waliambiwa *kumsujudia Adamu.* Lakini kwa desturi hakuna kiumbe cho chote kinachosujudiwa. Allah tu ndiye husujudiwa. Hivyo tumelifasiri neno hilo kwa namna ya mfano, *Mtiini Adamu.*

(2) Katika Qur'an Ibilisi anaonyeshwa kwamba aliumbwa kwa moto (sura 7:13) na pia inaelezwa kwamba alikuwa ni mmoja katika *Jinn* (Majinni), yaani viumbe wasioonekana (sura 18:51). Hivyo ilibidi asionekane kwa Adamu pia ambaye alikuwa sawa na wanadamu wote. Lakini Ibilisi anaonyeshwa kama aliyekuwa anazungumza na Adamu ana kwa ana. Hili laonyesha ya kwamba neno *Shaitaan* (Shetani) limetumiwa katika Aya ifuatayo kwa namna ya mfano, bila ya kukusudia yule Shetani anayewazengea watu kindanindani.

(3) Imeelezwa ya kwamba Adamu na mkewe walipokula mti uliokatazwa wakajiona wako uchi, hali hapa duniani hatuoni mti wo wote ambao mtu akiula anajiona yuko uchi. Hivyo "mti" na "uchi" tutayafasiri kwa maana ya mfano.

(4) Katika sura 20:119 tunaambiwa ya kwamba Allah alipomweka Adamu katika bustani alimwambia ya kuwa hutakuwa uchi humo. Lakini Aya 23 ya sura hii inasema Adamu akawa uchi. Hivyo moja katika habari hizi mbili italazimu ichukuliwe kwa maana ya methali, na hivyo tumefasiri neno "uchi" kwa maana ya "aibu," ambayo pia ni maana ya neno hilo la Kiarabu.

Maana iliyonyooka na nyepesi ya Aya hii, ni hii tu ya kwamba Malaika wanaamrishwa kumtii Adamu na kumsaidia katika kazi yake. Amri hii walipewa Malaika Adamu alipofanywa Mtume. Kwa kuwa mojawapo ya kazi za Malaika ni kuwanasihi watu kufanya matendo mema, basi waliambiwa kumsaidia Adamu kwa kuingiza mawazo mazuri katika nyoyo za watu na kuwanasihi

ثُمَّ لَاٰتِيَنَّهُمْ مِّنْۢ بَيْنِ اَيْدِيْهِمْ وَمِنْ خَلْفِهِمْ وَعَنْ اَيْمَانِهِمْ وَعَنْ شَمَآئِلِهِمْ ؕ وَلَا تَجِدُ اَكْثَرَهُمْ شٰكِرِيْنَ ﴿۱۸﴾

18. Kisha nitawafikia kutoka mbele yao na kutoka nyuma yao na kuume kwao na kushoto kwao; na Hutakuta wengi wao wenye kushukuru.

قَالَ اخْرُجْ مِنْهَا مَذْءُوْمًا مَّدْحُوْرًا ؕ لَمَنْ تَبِعَكَ مِنْهُمْ لَاَمْلَـَٔنَّ جَهَنَّمَ مِنْكُمْ اَجْمَعِيْنَ ﴿۱۹﴾

19. Akasema: Toka humo hali ya kudharauliwa na kufukuzwa. Atakae kufuata miongoni mwao, bila shaka nitaijaza Jahanamu kwa ninyi nyote.

وَيٰۤاٰدَمُ اسْكُنْ اَنْتَ وَزَوْجُكَ الْجَنَّةَ فَكُلَا مِنْ حَيْثُ شِئْتُمَا وَلَا تَقْرَبَا هٰذِهِ الشَّجَرَةَ فَتَكُوْنَا مِنَ الظّٰلِمِيْنَ ﴿۲۰﴾

20. Na ewe Adamu, kaa bustanini pamoja na mkeo, na kuleni mnapopenda, wala msiukaribie mti huu msije kuwa miongoni mwa wadhalimu.

فَوَسْوَسَ لَهُمَا الشَّيْطٰنُ لِيُبْدِيَ لَهُمَا مَا وٗرِيَ عَنْهُمَا مِنْ سَوْاٰتِهِمَا وَقَالَ مَا نَهٰىكُمَا رَبُّكُمَا عَنْ هٰذِهِ الشَّجَرَةِ اِلَّاۤ اَنْ تَكُوْنَا مَلَكَيْنِ اَوْ تَكُوْنَا مِنَ الْخٰلِدِيْنَ ﴿۲۱﴾

21. Lakini Shetani akawatia wasiwasi (mioyoni mwao) ili kuwadhihirishia aibu zao walizofichwa na akasema: Mola wenu Hakuwakatazeni bure mti huu, ila msije mkawa malaika wawili au miongoni mwa wakaao milele.

وَقَاسَمَهُمَاۤ اِنِّيْ لَكُمَا لَمِنَ النّٰصِحِيْنَ ﴿۲۲﴾

22. Naye akawaapia (kuwambia): Kwa yakini mimi ni mmoja wa watoao shauri jema kwenu.

---

kumkubali Adamu kwamba ni Mtume wa Mungu. Malaika mkuu ni Jibrili. Kadhalika roho zilizo ovu ambazo mkuu wao ni Ibilisi, hizo huwapa watu mashauri mabaya na kuwachochea wamwasi Mungu. Hivyo Malaika kwa kufuata amri ya Mungu wakamtii Adamu; na Ibilisi, mkuu wa roho zilizo ovu, akakataa kumtii na kumsaidia.

Aya 18. *Nitawafikia kutoka mbele yao na kutoka nyuma yao na kuume kwao na kushoto kwao*. Ni wazi Shetani hakusema nitawafikia kutoka juu yao na chini yao. Sababu yake ni hii ya kuwa mtu akinyenyekea kwa kujiangusha mbele ya Allah atapata msaada utokao juu, na rehema za Mungu zitamshukia na Shetani hataweza kumpoteza.

Aya 21. Kwa kuwa mahali alipowekwa Adamu, katika Qur'an pameitwa bustani kwa namna ya mfano, basi mfano huo unaendelezwa, na Adamu anasemwa kuwa alikatazwa kusogelea "mti", ambao hakika yake ni ukoo au kabila aliloambiwa ajiweke mbali nalo, kwa kuwa baadhi yao walikuwa maadui kwake.

Neno *Malakain* (malaika wawili) kwa *qir'a* nyingine husomwa *malikain*, yaani watawala wawili. *Qir'a* hiyo inaafikiana na sura 20:221, inayosema, *Basi Shetani akamtia wasiwasi, akasema, Ewe Adamu, je, nikujulishe mti wa milele na ufalme usiokoma?*

فَدَلّٰىهُمَا بِغُرُوْرٍ ۚ فَلَمَّا ذَاقَا الشَّجَرَةَ
بَدَتْ لَهُمَا سَوْاٰتُهُمَا وَطَفِقَا يَخْصِفٰنِ
عَلَيْهِمَا مِنْ وَّرَقِ الْجَنَّةِ ؕ وَنَادٰىهُمَا رَبُّهُمَآ
اَلَمْ اَنْهَكُمَا عَنْ تِلْكُمَا الشَّجَرَةِ وَاَقُلْ
لَّكُمَآ اِنَّ الشَّيْطٰنَ لَكُمَا عَدُوٌّ مُّبِيْنٌ ﴿٢٢﴾
قَالَا رَبَّنَا ظَلَمْنَآ اَنْفُسَنَا ۖ وَاِنْ لَّمْ
تَغْفِرْ لَنَا وَتَرْحَمْنَا لَنَكُوْنَنَّ مِنَ
الْخٰسِرِيْنَ ﴿٢٣﴾

23. Basi akawakengeusha wote wawili kwa udanganyifu; na walipoonja mti ule, aibu zao zikawadhihirikia na wakaanza kujibandika majani ya bustani; na Mola wako Akawaita: Je, sikuwakatazeni mti huo na kuwaambieni ya kwamba Shetani ni adui yenu dhahiri?

24. Wakasema: Mola wetu, tumedhulumu nafsi zetu; na kama Hutusamehe na kuturehemu, bila shaka tutakuwa miongoni mwa wenye hasara.

Mtu mwovu, ambaye hapa anaitwa Shetani, alifanya hila yake namna hii:- Alimfikia Adamu na akamwambia ya kuwa, sababu iliyomfanya Allah akukataze kuwa na neno na ukoo ule ni kwamba wao ni maadui zako, wanaweza kufanya hila ya kukuangusha kama ungekurubiana nao. Lakini, kwa kuwa ukoo huo sasa wanaonyesha urafiki kwako, basi hakuna tena hatari. Si hivyo tu, bali ukoo huo unaweza kuwa njia ya wewe kupata nguvu. Akateta ya kwamba makatazo ya Allah hayakukusudiwa kwa nyakati zote, yalikusudiwa kwa wakati maalumu tu, na maadamu sababu zilizofanya ukatazwe sasa haziko, na makatazo pia yamekwisha.

Kwa njia hii huyu Shetani akafanikiwa kumdanganya Adamu na akamhakikishia kwa kiapo ya kuwa yeye ni nasihi wake (sura 7:22). Adamu akababaika na akashawishika kufikiri ya kwamba, maadamu sababu ya kukatazwa kwake zimekoma, basi makatazo pia yamekoma. Hilo lilikuwa ni kosa katika kukata shauri, naye hakuwa amekusudia kuasi amri ya Allah. Mahali pengine Qur'an inasema, *Adamu akasahau, nasi Hatukumwona mwenye nia (ya kuasi)* (sura 20:116).

Aya 23. *Sauaatuhumaa*"Aibu zao." Sauaat ni wingi wa neno *sauah,* ambalo limetokana na neno *saa-a* lenye maana, ilikuwa ovu, mbaya au ichukizayo. *Sauah* maana yake ni uovu wo wote; ubaya; neno lisilofaa; tendo, tabia au mwenendo unaochukiza: neno au tendo ambalo mtu analionea haya linapotokea na ambalo angependa alifiche; tendo au kitu cho chote kinachoaibisha; viungo vya nje vya uzazi vya mwanamume au mwanamke; mkundu; maiti au mwili uliokufa (Akrab na Lane). Neno hili pia hutumiwa kutaja aibu za mtu zinazofichama ndani yake.

Adamu na mkewe kudhihirikiwa na aibu zao kunakotajwa na Aya hii, sio mradi wake kwamba walibaki utupu, maana hakuna uchi wa mtu ye yote ulifichika kwake mwenyewe; bali ni kwamba baadhi ya upungufu na udhaifu wao walikuwa hawaujui mpaka adui yao alipowaghuri na kuwatoa mahali pao pa salama. Kabla ya jambo hili Adamu alifanya kazi yake akisaidiwa na fadhili za Allah zilizoendelea kuziba na kufunika upungufu wake na udhaifu wake; lakini alipofanya itifaki na ukoo aliokatazwa, akawa kweupe na akasikitika jinsi alivyokuwa dhaifu.

Kwa kuwa Shetani alifanikiwa kuingiza mfarakano katika wafuasi wa Adamu, na waliokuwa na imani dhaifu miongoni mwao wakatoka, Nabii Adamu akaanza kukusanya *auraaq* (majani) ya bustani, yaani vijana katika wafusi wake (Akrab, Lane, Lisan), na akaanza kuwaunganisha na kuwatia umoja watu wake kwa msaada wa vijana hao. Kwa desturi vijana huwa hawana upendeleo na kujali hatari ambao huwafuata Mitume wa Mungu na kuwasaidia.

Aya 24. Adamu hakuendelea muda mrefu katika kosa. Mara alitambua alivyodanganyika na akafanya haraka kuelekea kwa Allah ili kutubu.

قَالَ اهْبِطُوْا بَعْضُكُمْ لِبَعْضٍ عَدُوٌّ ۚ وَلَكُمْ فِي الْاَرْضِ مُسْتَقَرٌّ وَّمَتَاعٌ اِلٰى حِيْنٍ ﴿٢٥﴾

25. Akasema: Nendeni, ninyi kwa ninyi m maadui. Na kao lenu litakuwa katika ardhi na manufaa kwa muda.

قَالَ فِيْهَا تَحْيَوْنَ وَفِيْهَا تَمُوْتُوْنَ وَمِنْهَا تُخْرَجُوْنَ ﴿٢٦﴾ ع

26. Akasema: Mtaishi humo na mtafia humo, na mtatolewa humo.

FUNGU 3

يٰبَنِيْٓ اٰدَمَ قَدْ اَنْزَلْنَا عَلَيْكُمْ لِبَاسًا يُّوَارِيْ سَوْاٰتِكُمْ وَرِيْشًا ؕ وَلِبَاسُ التَّقْوٰى ۙ ذٰلِكَ خَيْرٌ ؕ ذٰلِكَ مِنْ اٰيٰتِ اللّٰهِ لَعَلَّهُمْ يَذَّكَّرُوْنَ ﴿٢٧﴾

27. Enyi wanadamu, hakika Tumewateremshieni nguo zifichazo aibu zenu na mapambo; na nguo za utawa ndizo bora. Hizo ni katika Ishara za Allah ili wapate kushika mawaidha.

يٰبَنِيْٓ اٰدَمَ لَا يَفْتِنَنَّكُمُ الشَّيْطٰنُ كَمَآ اَخْرَجَ اَبَوَيْكُمْ مِّنَ الْجَنَّةِ يَنْزِعُ عَنْهُمَا لِبَاسَهُمَا لِيُرِيَهُمَا سَوْاٰتِهِمَا ؕ اِنَّهٗ يَرٰىكُمْ هُوَ وَقَبِيْلُهٗ مِنْ حَيْثُ لَا تَرَوْنَهُمْ ؕ اِنَّا جَعَلْنَا الشَّيٰطِيْنَ اَوْلِيَآءَ لِلَّذِيْنَ لَا يُؤْمِنُوْنَ ﴿٢٨﴾

28. Enyi wanadamu, Shetani asiwatieni katika fitina, kama alivyowatoa baba zenu katika bustani kwa kuwavua nguo zao ili kuwaonyesha aibu zao. Hakika yeye anawaoneni pamoja na kabila lake kwa mahali msipowaona. Bila shaka Sisi Tumewajaalia mashetani kuwa rafiki wa wale wasioamini.

وَاِذَا فَعَلُوْا فَاحِشَةً قَالُوْا وَجَدْنَا عَلَيْهَآ اٰبَآءَنَا وَاللّٰهُ اَمَرَنَا بِهَا ؕ قُلْ اِنَّ اللّٰهَ لَا يَاْمُرُ بِالْفَحْشَآءِ ؕ اَتَقُوْلُوْنَ عَلَى اللّٰهِ مَا لَا تَعْلَمُوْنَ ﴿٢٩﴾

29. Na wanapofanya mambo ya aibu husema: Tuliwakuta baba zetu juu ya hayo na (pia) Allah Ametuamuru hayo. Sema: Hakika Allah haamuru mambo ya aibu. Je, mnasema juu ya Allah msiyoyajua?

Aya 25. Aya hii inaonyesha ya kuwa Adamu aliamrishwa kuhama nchi aliyozaliwa kwa sababu kulitokea uadui baina ya watu wake. Jambo hili linazidi kuonyesha ya kwamba "bustani" aliyoambiwa kuitoka haikuwa Pepo ya mbinguni, maana Qur'an inasema, mtu akisha ingia Peponi hatoki (sura 15:49), wala Shetani hawezi kumsogelea au kumdanganya mtu aliye Peponi.

Aya 26. Aya hii inaonyesha kanuni ya Allah ya kwamba mwanadamu lazima aishi hapa hapa ardhini, na afe hapa hapa, na ya kwamba haiwezekani mtu akakae mbinguni na kiwiliwili chake.

Aya 27. Aya hii inaonyesha makusudio mawili kwa ajili ya kutumia nguo. (1) Kuficha uchi wetu na (2) kuwa mapambo na kutufanya tupendeze. Lakini siku hizi ni jambo la kusikitisha ya kwamba nguo zinaendelea kuwa zinaachwa na wanawake wa pande za Magharibi, na ugonjwa huu sasa unaenea upesi upesi pande za Mashariki na Afrika.

قُلْ اَمَرَ رَبِّیْ بِالْقِسْطِ ۫ وَ اَقِیْمُوْا
وُجُوْهَكُمْ عِنْدَ كُلِّ مَسْجِدٍ وَّادْعُوْهُ
مُخْلِصِیْنَ لَهُ الدِّیْنَ ؕ كَمَا بَدَاَكُمْ
تَعُوْدُوْنَ ﴿۲۹﴾

30. Sema: Mola wangu Ameamuru uadilifu. Na rekebisheni mielekeo yenu ndani ya kila msikiti na mumuombe Yeye kwa utii halisi. Kama Alivyowaumbeni kwanza ndivyo mtarudi.

فَرِیْقًا هَدٰی وَ فَرِیْقًا حَقَّ عَلَیْهِمُ الضَّلٰلَةُ ؕ
اِنَّهُمُ اتَّخَذُوا الشَّیٰطِیْنَ اَوْلِیَآءَ مِنْ دُوْنِ
اللّٰهِ وَیَحْسَبُوْنَ اَنَّهُمْ مُّهْتَدُوْنَ ﴿۳۰﴾

31. Ameliongoza kundi moja na kundi jingine upotevu umehakiki juu yao; kwa hakika waliwafanya mashetani kuwa marafiki (wao) badala ya Allah, na wanadhani ya kuwa wao wameongoka.

یٰبَنِیْۤ اٰدَمَ خُذُوْا زِیْنَتَكُمْ عِنْدَ كُلِّ مَسْجِدٍ
وَّكُلُوْا وَاشْرَبُوْا وَلَا تُسْرِفُوْا ۚ اِنَّهٗ لَا یُحِبُّ
الْمُسْرِفِیْنَ ﴿۳۱﴾ ع

32. Enyi wanadamu, shikeni ma pambo yenu kwenye kila msikiti; na kuleni na kunyweni wala msipite kiasi; hakika Yeye Hawapendi wapitao kiasi.

FUNGU 4

قُلْ مَنْ حَرَّمَ زِیْنَةَ اللّٰهِ الَّتِیْۤ اَخْرَجَ لِعِبَادِهٖ
وَالطَّیِّبٰتِ مِنَ الرِّزْقِ ؕ قُلْ هِیَ لِلَّذِیْنَ
اٰمَنُوْا فِی الْحَیٰوةِ الدُّنْیَا خَالِصَةً یَّوْمَ الْقِیٰمَةِ ؕ
كَذٰلِكَ نُفَصِّلُ الْاٰیٰتِ لِقَوْمٍ یَّعْلَمُوْنَ ﴿۳۲﴾

33. Sema: Ni nani aliyeharamisha mapambo ya Allah ambayo Amewatolea watu Wake, na vitu vizuri vya riziki? Sema: hivyo ni kwa waaminio katika maisha ya dunia, (na) hasa siku ya Kiyama. Hivi ndivyo Tunavyozieleza Aya kwa watu wajuao.

قُلْ اِنَّمَا حَرَّمَ رَبِّیَ الْفَوَاحِشَ مَا ظَهَرَ
مِنْهَا وَمَا بَطَنَ وَالْاِثْمَ وَالْبَغْیَ بِغَیْرِ الْحَقِّ
وَاَنْ تُشْرِكُوْا بِاللّٰهِ مَا لَمْ یُنَزِّلْ بِهٖ سُلْطٰنًا
وَّاَنْ تَقُوْلُوْا عَلَی اللّٰهِ مَا لَا تَعْلَمُوْنَ ﴿۳۳﴾

34. Sema: Hakika Mola wangu Ameharamisha mambo ya aibu, yaliyodhihirika na yaliyofichika, na dhambi na uasi pasipo haki, na kumshirikisha Allah na ambacho Hakukiteremshia dalili, na kusema juu ya Allah msiyoyajua.

Aya 30. *Masjid.* neno hili maana yake ni mahali mtu anapoabudia; mahali mtu anaposalia; nyumba ya kusalia; msikiti (Lane) Linapokuwa *ismu dharf* maana yake linakuwa wakati wa Sala kama tulivyolifasiri hapa (Baidhawi).

Aya 32. Aya hii inawaamuru Waislamu waende kusali au waende msikitini kufanya ibada katika hali ya kujipamba vizuri na usafi. Mtume *s.a.w.* aliwakataza watu kwenda kusali msikitini baada ya kula kitunguu, ili harufu mbaya isiwachukize wengine. Kadhalika akawaamrisha watu waoge mara kwa mara na hasa kabla ya Sala ya Ijumaa. Na katika hadithi zingine imejulikana kuwa usafi ni sharti kubwa ya ibada.

وَلِكُلِّ اُمَّةٍ اَجَلٌ ۚ فَاِذَا جَآءَ اَجَلُهُمْ لَا
يَسْتَاْخِرُوْنَ سَاعَةً وَّلَا يَسْتَقْدِمُوْنَ ﴿٣٥﴾

35. Na kila umati una muda. Basi utakapowafikia muda wao hawatakawia hata saa moja wala hawatatangulia.

يٰبَنِيْٓ اٰدَمَ اِمَّا يَاْتِيَنَّكُمْ رُسُلٌ مِّنْكُمْ
يَقُصُّوْنَ عَلَيْكُمْ اٰيٰتِيْ ۙ فَمَنِ اتَّقٰى وَاَصْلَحَ
فَلَا خَوْفٌ عَلَيْهِمْ وَلَا هُمْ يَحْزَنُوْنَ ﴿٣٦﴾

36. Enyi wanadamu, wakikufikieni, (na bila shaka watawafikieni), Mitume kutoka miongoni mwenu, watawaelezeni Aya Zangu. Basi atakayeogopa na ku - fanya wema, haitakuwa hofu juu yao, wala hawatahuzunika.

وَالَّذِيْنَ كَذَّبُوْا بِاٰيٰتِنَا وَاسْتَكْبَرُوْا
عَنْهَآ اُولٰٓئِكَ اَصْحٰبُ النَّارِ ۚ هُمْ فِيْهَا
خٰلِدُوْنَ ﴿٣٧﴾

37. Na wale wanaokadhibisha Ishara Zetu na kuzifanyia kiburi hao ndio watu wa Motoni, watakaa humo.

فَمَنْ اَظْلَمُ مِمَّنِ افْتَرٰى عَلَى اللّٰهِ كَذِبًا
اَوْ كَذَّبَ بِاٰيٰتِهٖ ؕ اُولٰٓئِكَ يَنَالُهُمْ نَصِيْبُهُمْ
مِّنَ الْكِتٰبِ ؕ حَتّٰٓى اِذَا جَآءَتْهُمْ رُسُلُنَا
يَتَوَفَّوْنَهُمْ ۙ قَالُوْٓا اَيْنَ مَا كُنْتُمْ تَدْعُوْنَ
مِنْ دُوْنِ اللّٰهِ ؕ قَالُوْا ضَلُّوْا عَنَّا وَشَهِدُوْا
عَلٰٓى اَنْفُسِهِمْ اَنَّهُمْ كَانُوْا كٰفِرِيْنَ ﴿٣٨﴾

38. Basi ni nani mdhalimu mkubwa kuliko yule anayemtungia uwongo Al - lah au anazikadhibisha Ishara Zake? Hao ndio ambao itawafikia sehemu yao ya Kitabu, mpaka watakapowafikia Wajumbe wetu kuwafisha, watasema: Wako wapi mliokuwa mkiwaita badala ya Allah? Watasema: Wametupotea; na watajishuhudia wenyewe kwamba hakika walikuwa makafiri.

قَالَ ادْخُلُوْا فِيْٓ اُمَمٍ قَدْ خَلَتْ مِنْ قَبْلِكُمْ
مِّنَ الْجِنِّ وَالْاِنْسِ فِي النَّارِ ؕ كُلَّمَا دَخَلَتْ
اُمَّةٌ لَّعَنَتْ اُخْتَهَا ؕ حَتّٰٓى اِذَا ادَّارَكُوْا
فِيْهَا جَمِيْعًا ۙ قَالَتْ اُخْرٰىهُمْ لِاُوْلٰىهُمْ
رَبَّنَا هٰٓؤُلَآءِ اَضَلُّوْنَا فَاٰتِهِمْ عَذَابًا
ضِعْفًا مِّنَ النَّارِ ؕ قَالَ لِكُلٍّ ضِعْفٌ
وَّلٰكِنْ لَّا تَعْلَمُوْنَ ﴿٣٩﴾

39. Atasema: Ingieni Motoni pamoja na umati uliopita kabla yenu wa ma - jini na watu, kila utakapoingia umati utawalaani wenzao, mpaka watakapoku - sanyika wote humo, wa nyuma wao watasema kwa ajili ya wa kwanza wao: Mola wetu hawa ndio waliotupoteza, basi Uwape adhabu ya Moto maradufu. Atasema: Kwa ninyi nyote ni (adhabu) maradufu, lakini ninyi hamjui.

Aya 36. Aya hii pia inaweza kufasiriwa, *Kama watawafikieni Mitume*. Kwa tafsiri hii haitakuwa mradi wake kwamba Mitume wanaweza au hawawezi kufika. Bali inafanana na sura 2:39 isemayo, *Kama utawafikieni mwongozo kutoka Kwangu;* ambayo haitakuwa kamwe mradi wake kudhania kuwa pengine mwongozo hauwezi kufika. Neno immaa linakusudiwa kuonyesha ya kuwa kama mtapata kuwa katika wakati ambao Mjumbe wa Mungu ametokea, msikose kumkubali.

وَقَالَتْ اُوْلٰىهُمْ لِاُخْرٰىهُمْ فَمَا كَانَ لَكُمْ عَلَيْنَا مِنْ فَضْلٍ فَذُوْقُوا الْعَذَابَ بِمَا كُنْتُمْ تَكْسِبُوْنَ ﴿٣٩﴾

40. Na wa kwanza wao watasema kwa wengine wao: Basi ninyi pia hamkuwa na fadhili kuliko sisi! kwa hiyo onjeni adhabu kwa sababu ya yale mliyokuwa mkiyachuma.

FUNGU 5

اِنَّ الَّذِيْنَ كَذَّبُوْا بِاٰيٰتِنَا وَاسْتَكْبَرُوْا عَنْهَا لَا تُفَتَّحُ لَهُمْ اَبْوَابُ السَّمَآءِ وَلَا يَدْخُلُوْنَ الْجَنَّةَ حَتّٰى يَلِجَ الْجَمَلُ فِىْ سَمِّ الْخِيَاطِ ؕ وَكَذٰلِكَ نَجْزِى الْمُجْرِمِيْنَ ﴿٤٠﴾

41. Hakika wale waliokadhibisha Aya Zetu na kuzifanyia kiburi, hawatafunguliwa milango ya mbingu, wala hawataingia Peponi mpaka aingie ngamia katika tundu la sindano; na hivi ndivyo Tunavyowalipa wakosefu.

لَهُمْ مِّنْ جَهَنَّمَ مِهَادٌ وَّمِنْ فَوْقِهِمْ غَوَاشٍ ؕ وَكَذٰلِكَ نَجْزِى الظّٰلِمِيْنَ ﴿٤١﴾

42. Watakuwa na kitanda cha Jahannamu na vifuniko (vyake) juu yao; na hivi ndivyo Tunavyowalipa wadhalimu.

وَالَّذِيْنَ اٰمَنُوْا وَعَمِلُوا الصّٰلِحٰتِ لَا نُكَلِّفُ نَفْسًا اِلَّا وُسْعَهَآ ۚ اُولٰٓئِكَ اَصْحٰبُ الْجَنَّةِ ۚ هُمْ فِيْهَا خٰلِدُوْنَ ﴿٤٢﴾

43. Na wale walioamini na kufanya vitendo vizuri - Hatuikalifishi nafsi yo yote ila kwa wasaa wake - hao ndio watu wa Peponi, wao watakaa humo.

وَنَزَعْنَا مَا فِىْ صُدُوْرِهِمْ مِّنْ غِلٍّ تَجْرِىْ مِنْ تَحْتِهِمُ الْاَنْهٰرُ ۚ وَقَالُوا الْحَمْدُ لِلّٰهِ الَّذِىْ هَدٰىنَا لِهٰذَا ۫ وَمَا كُنَّا لِنَهْتَدِىَ لَوْلَآ اَنْ هَدٰىنَا اللّٰهُ ۚ لَقَدْ جَآءَتْ رُسُلُ رَبِّنَا بِالْحَقِّ ؕ وَنُوْدُوْٓا اَنْ تِلْكُمُ الْجَنَّةُ اُوْرِثْتُمُوْهَا بِمَا كُنْتُمْ تَعْمَلُوْنَ ﴿٤٣﴾

44. Na Tutaiondoa chuki yote vifuani mwao; chini yao itapita mito, na watasema: Sifa zote njema zinamhusu Allah Ambaye Ametuongoza kwenye haya. Na hatukuwa wenye kuongoka wenyewe kama Asingetuongoza Allah. Bila shaka Mitume wa Mola wetu walileta haki. Na watanadiwa ya kwamba hii ndio Pepo mliyorithishwa kwa sababu ya yale mliyokuwa mkifanya.

Maneno haya, *watawaeleza Aya Zangu,* yanaonyesha kwamba Mitume watakaofika baada ya Mtume Muhammad *s.a.w.* hawataleta Sheria mpya, bali watafuata Sheria ya Uislamu na kazi yao itakuwa kuwaeleza watu Aya za Qur'an.

Aya 41. *Aingie ngamia katika tundu la sindano.* Yaani kama vile haiwezekani ngamia kuingia katika tundu la sindano, kadhalika haiwezekani watu wabaya kuingia Peponi.

وَنَادٰٓى اَصْحٰبُ الْجَنَّةِ اَصْحٰبَ النَّارِ اَنْ
قَدْ وَجَدْنَا مَا وَعَدَنَا رَبُّنَا حَقًّا فَهَلْ
وَجَدْتُّمْ مَّا وَعَدَ رَبُّكُمْ حَقًّا ؕ قَالُوْا نَعَمْ ۚ
فَاَذَّنَ مُؤَذِّنٌۢ بَيْنَهُمْ اَنْ لَّعْنَةُ اللّٰهِ عَلَى
الظّٰلِمِيْنَ ۙ﴿۴۵﴾

45. Na watu wa Peponi watawaita watu wa Motoni (kuwaambia): Bila shaka sisi tumekuta Aliyotuahidi Mola wetu kuwa kweli. Je, nanyi pia mmekuta Aliyowaahidini Mola wenu kuwa kweli? Watasema: Ndio. Basi mtangazaji atatangaza kati yao: Laana ya Allah iko juu ya wadhalimu.

الَّذِيْنَ يَصُدُّوْنَ عَنْ سَبِيْلِ اللّٰهِ وَيَبْغُوْنَهَا
عِوَجًا ۚ وَهُمْ بِالْاٰخِرَةِ كٰفِرُوْنَ ۘ﴿۴۵﴾

46. Ambao wanazuilia njia ya Allah na wanataka kuipotosha, nao ni wenye kuikataa Akhera.

وَبَيْنَهُمَا حِجَابٌ ۚ وَعَلَى الْاَعْرَافِ
رِجَالٌ يَّعْرِفُوْنَ كُلًّا ۢ بِسِيْمٰهُمْ ۚ وَنَادَوْا
اَصْحٰبَ الْجَنَّةِ اَنْ سَلٰمٌ عَلَيْكُمْ ۟
لَمْ يَدْخُلُوْهَا وَهُمْ يَطْمَعُوْنَ ﴿۴۶﴾

47. Na kati yao hao wawili itakuwa pazia. Na juu ya mahali palipoinuka patakuwa watu watakaowafahamu wote kwa alama zao, na watawaita watu wa Peponi (kuwaambia): Iwe amani juu yenu: hawajaingia nao wanatamani.

وَاِذَا صُرِفَتْ اَبْصَارُهُمْ تِلْقَآءَ
اَصْحٰبِ النَّارِ ۙ قَالُوْا رَبَّنَا لَا تَجْعَلْنَا مَعَ
الْقَوْمِ الظّٰلِمِيْنَ ﴿۴۷﴾ ع ۱۳

48. Na macho yao yatakapogeuzwa kwenye watu wa Motoni watasema: Mola wetu usituweke pamoja na watu wadhalimu.

FUNGU 6

وَنَادٰٓى اَصْحٰبُ الْاَعْرَافِ رِجَالًا
يَّعْرِفُوْنَهُمْ بِسِيْمٰهُمْ قَالُوْا مَآ اَغْنٰى
عَنْكُمْ جَمْعُكُمْ وَمَا كُنْتُمْ
تَسْتَكْبِرُوْنَ ﴿۴۸﴾

49. Na watu wa mahali paliponyanyuka watawaita watu wanaowafahamu kwa alama zao, watasema: Haikuwafaidisheni jamii yenu wala mlivyokuwa mkijivunia.

اَهٰٓؤُلَآءِ الَّذِيْنَ اَقْسَمْتُمْ لَا يَنَالُهُمُ اللّٰهُ
بِرَحْمَةٍ ؕ اُدْخُلُوا الْجَنَّةَ لَا خَوْفٌ
عَلَيْكُمْ وَلَآ اَنْتُمْ تَحْزَنُوْنَ ﴿۴۹﴾

50. Je, hawa ndio wale mliokuwa mkiwaapia kwamba Allah Hatawafikishia rehema? Ingieni Peponi, hakuna hofu juu yenu, wala hamtahuzunika.

وَنَادٰٓى اَصْحٰبُ النَّارِ اَصْحٰبَ الْجَنَّةِ اَنْ
اَفِيْضُوْا عَلَيْنَا مِنَ الْمَآءِ اَوْ مِمَّا رَزَقَكُمُ اللّٰهُ ؕ
قَالُوْٓا اِنَّ اللّٰهَ حَرَّمَهُمَا عَلَى الْكٰفِرِيْنَ ۙ﴿۵۰﴾

51. Na watu wa Motoni watawaita watu wa Peponi, (kuwaambia): Mtupatie maji au katika vile Alivyowapeni Allah. Watasema: Hakika Allah Ameviharamisha vyote viwili kwa makafiri.

الَّذِيْنَ اتَّخَذُوْا دِيْنَهُمْ لَهْوًا وَّ لَعِبًا
وَّغَرَّتْهُمُ الْحَيٰوةُ الدُّنْيَا ۚ فَالْيَوْمَ نَنْسٰىهُمْ
كَمَا نَسُوْا لِقَآءَ يَوْمِهِمْ هٰذَا ۙ وَمَا كَانُوْا
بِاٰيٰتِنَا يَجْحَدُوْنَ ﴿٥١﴾

52. Ambao waliifanya dini yao kuwa upuuzi na mchezo, na maisha ya dunia yakawadanganya. Basi leo Sisi tunawasahau kama walivyousahau mkutano wa Siku yao hii, na sababu walikuwa wakizikataa Aya Zetu.

وَلَقَدْ جِئْنٰهُمْ بِكِتٰبٍ فَصَّلْنٰهُ عَلٰى عِلْمٍ
هُدًى وَّ رَحْمَةً لِّقَوْمٍ يُّؤْمِنُوْنَ ﴿٥٢﴾

53. Na bila shaka Tumewaletea Kitabu Tulichokibainisha kwa elimu, mwongozo na rehema kwa watu waaminio.

هَلْ يَنْظُرُوْنَ اِلَّا تَاْوِيْلَهٗ ؕ يَوْمَ يَاْتِيْ
تَاْوِيْلُهٗ يَقُوْلُ الَّذِيْنَ نَسُوْهُ مِنْ قَبْلُ قَدْ
جَآءَتْ رُسُلُ رَبِّنَا بِالْحَقِّ ۚ فَهَلْ لَّنَا مِنْ
شُفَعَآءَ فَيَشْفَعُوْا لَنَآ اَوْ نُرَدُّ فَنَعْمَلَ
غَيْرَ الَّذِيْ كُنَّا نَعْمَلُ ؕ قَدْ خَسِرُوْٓا
اَنْفُسَهُمْ وَضَلَّ عَنْهُمْ مَّا كَانُوْا
يَفْتَرُوْنَ ﴿٥٣﴾ ع

54. Hawatazamii ila matokeo yake ya mwisho. Siku yatakapotokea matokeo yake, watasema wale walioisahau zamani: Hakika Mitume wa Mola wetu wameleta haki, Je, tunao waombezi ili watuombee? Au turudishwe ili tufanye ghairi ya yale tuliyokuwa tukifanya? Bila shaka wamezitia nafsi zao hasarani, na yamewapotea waliyokuwa wakiyatunga.

FUNGU 7

اِنَّ رَبَّكُمُ اللّٰهُ الَّذِيْ خَلَقَ السَّمٰوٰتِ
وَالْاَرْضَ فِيْ سِتَّةِ اَيَّامٍ ثُمَّ اسْتَوٰى عَلَى
الْعَرْشِ ۟ يُغْشِي الَّيْلَ النَّهَارَ يَطْلُبُهٗ
حَثِيْثًا ۙ وَّ الشَّمْسَ وَالْقَمَرَ وَالنُّجُوْمَ
مُسَخَّرٰتٍ بِاَمْرِهٖ ؕ اَلَا لَهُ الْخَلْقُ
وَالْاَمْرُ ؕ تَبٰرَكَ اللّٰهُ رَبُّ الْعٰلَمِيْنَ ﴿٥٤﴾

55. Hakika Mola wenu ni Allah Aliyeziumba mbingu na ardhi katika nyakati sita, kisha Akastawi juu ya Arshi. Huufunika usiku kwa mchana uufuatao upesi· Na jua na mwezi na nyota vilivyotiishwa kwa amri Yake. Fahamuni! uumbaji na amri ni Vyake. Mwenye baraka ni Allah, Mola wa walimwengu.

Aya 53. Kitabu kilichotajwa hapa ni Qur'an ambacho kina mambo matatu: - (1) "Elimu" iliyo ya lazima kumwezesha mtu amjue Allah. (2) "Mwongozo" unaomwezesha mtu kutimiza wajibu wake kwa Allah na kuangalia haki za watu. (3) "Rehema" au huruma ya Allah inayowashukia waaminio.

Aya 55. *Nyakati sita.* Hapa neno *Ayyam* maana yake ni "nyakati." Kadhalika maana ya neno hili ni "siku" ya saa 24 (Akrab). Hizi siku zetu zinahesabiwa na jua, lakini Allah alipoumba mbingu na ardhi, jua pia liliumbwa pamoja navyo. Hivyo, *ayyaam* hizo hazikuwa za jua kutoka na kutua, bali ni nyakati tu. Pia nyakati hizo sita zinaweza kuwa muda wa miaka mingi sana hata maelfu (sura 70:5).

56. Mwombeni Mola wenu kwa unyenyekevu na kwa siri. Hakika Yeye Hawapendi warukao mipaka.

اُدْعُوْا رَبَّكُمْ تَضَرُّعًا وَّخُفْيَةً ؕ اِنَّهٗ لَا يُحِبُّ الْمُعْتَدِيْنَ ﴿۵۶﴾

57. Wala msifanye uharibifu katika ardhi ikiisha tulia. Na Mwombeni kwa kuogopa na kwa kutumai. Bila shaka rehema za Allah zi karibu na wafanyao hisani.

وَلَا تُفْسِدُوْا فِى الْاَرْضِ بَعْدَ اِصْلَاحِهَا وَادْعُوْهُ خَوْفًا وَّطَمَعًا ؕ اِنَّ رَحْمَتَ اللّٰهِ قَرِيْبٌ مِّنَ الْمُحْسِنِيْنَ ﴿۵۷﴾

58. Na Yeye ndiye Apelekaye pepo kuwa habari njema mbele ya rehema Zake, hata zinapobeba mawingu mazito Tunayasukuma kwenye mji ulikokufa, kisha Tunateremsha maji kwa hayo, na kwayo Tunaotesha kila aina ya matunda. Hivi ndivyo tunavyowafufua wafu ili mpate kukumbuka.

وَهُوَ الَّذِىْ يُرْسِلُ الرِّيٰحَ بُشْرًا بَيْنَ يَدَىْ رَحْمَتِهٖ ؕ حَتّٰۤى اِذَاۤ اَقَلَّتْ سَحَابًا ثِقَالًا سُقْنٰهُ لِبَلَدٍ مَّيِّتٍ فَاَنْزَلْنَا بِهِ الْمَآءَ فَاَخْرَجْنَا بِهٖ مِنْ كُلِّ الثَّمَرٰتِ ؕ كَذٰلِكَ نُخْرِجُ الْمَوْتٰى لَعَلَّكُمْ تَذَكَّرُوْنَ ﴿۵۸﴾

59. Na nchi nzuri huota mimea yake kwa idhini ya Mola wake, na iliyo mbaya haitoi ila mbaya tu. Hivi ndivyo Tunavyoeleza Ishara kwa watu wanaoshukuru.

وَالْبَلَدُ الطَّيِّبُ يَخْرُجُ نَبَاتُهٗ بِاِذْنِ رَبِّهٖ ۚ وَالَّذِىْ خَبُثَ لَا يَخْرُجُ اِلَّا نَكِدًا ؕ كَذٰلِكَ نُصَرِّفُ الْاٰيٰتِ لِقَوْمٍ يَّشْكُرُوْنَ ﴿۵۹﴾ ع ۚ ۱۴

FUNGU 8

60. Hakika Tulimtuma Nuhu kwa watu wake, naye akasema: Enyi watu wangu, mwabuduni Allah, ninyi hamna mungu ghairi Yake; hakika mimi ninawahofieni adhabu ya siku iliyo kuu.

لَقَدْ اَرْسَلْنَا نُوْحًا اِلٰى قَوْمِهٖ فَقَالَ يٰقَوْمِ اعْبُدُوا اللّٰهَ مَا لَكُمْ مِّنْ اِلٰهٍ غَيْرُهٗ ؕ اِنِّىْۤ اَخَافُ عَلَيْكُمْ عَذَابَ يَوْمٍ عَظِيْمٍ ﴿۶۰﴾

Aya 57. *Wafanyao hisani.* Neno *Muhsin* (afanyaye hisani) maana yake ni mtu anayefanya bidii kuwa mkamilifu katika vitendo vyake. Hadithi ya Mtume *s.a.w.* inaeleza kuwa Muhsin ni mtu anayefanya tendo jema kana kwamba anamwona Mungu; au kwa akali ajue kuwa Mungu anamwona (Bukhari *Kitaabul-Iiman*).

Aya 60. *Nuuh* ni Nabii wa kale kabisa ambaye Biblia inatuambia alikuwako vilipopita vizazi tisa baada ya Adamu na vizazi kumi na moja kabla ya Ibrahimu (Mwanzo 5:3-32; Luka 3:34-38). Kwao ni nchi ya Mesopotamia.

Adhabu ya siku iliyo kuu. Siku iliyo kuu mradi wake ni siku ya adhabu nzito ya kutisha mno ambayo haiwezi kusahauliwa.

قَالَ الْمَلَاُ مِنْ قَوْمِهٖٓ اِنَّا لَنَرٰىكَ فِيْ ضَلٰلٍ مُّبِيْنٍ ﴿٦١﴾

61. Wakuu wa watu wake wakasema: Kwa yakini tunakuona umo katika upotevu dhahiri.

قَالَ يٰقَوْمِ لَيْسَ بِيْ ضَلٰلَةٌ وَّلٰكِنِّيْ رَسُوْلٌ مِّنْ رَّبِّ الْعٰلَمِيْنَ ﴿٦٢﴾

62. Akasema: Enyi kaumu yangu, mimi simo katika upotevu, lakini mimi ni Mtume nitokaye kwa Mola wa walimwengu.

اُبَلِّغُكُمْ رِسٰلٰتِ رَبِّيْ وَاَنْصَحُ لَكُمْ وَاَعْلَمُ مِنَ اللّٰهِ مَا لَا تَعْلَمُوْنَ ﴿٦٣﴾

63. Nawafikishieni risala za Mola wangu na ninawasihini na ninayajua kutoka kwa Allah msiyoyajua.

اَوَعَجِبْتُمْ اَنْ جَآءَكُمْ ذِكْرٌ مِّنْ رَّبِّكُمْ عَلٰى رَجُلٍ مِّنْكُمْ لِيُنْذِرَكُمْ وَلِتَتَّقُوْا وَلَعَلَّكُمْ تُرْحَمُوْنَ ﴿٦٤﴾

64. Je! mnastaajabu kuwafikieni mawaidha kutoka kwa Mola wenu kwa njia ya mtu aliye ni mmoja wenu, ili awaonyeni na ili muogope na mpate kurehemiwa?

فَكَذَّبُوْهُ فَاَنْجَيْنٰهُ وَالَّذِيْنَ مَعَهٗ فِي الْفُلْكِ وَاَغْرَقْنَا الَّذِيْنَ كَذَّبُوْا بِاٰيٰتِنَا ؕ اِنَّهُمْ كَانُوْا قَوْمًا عَمِيْنَ ﴿٦٥﴾ ع

65. Lakini walimkadhibisha; basi Tukamuokoa yeye na waliokuwa pamoja naye katika safina, na Tukawazamisha wale waliozikadhibisha Aya Zetu. Bila shaka hao walikuwa watu vipofu.

FUNGU 9

وَاِلٰى عَادٍ اَخَاهُمْ هُوْدًا ؕ قَالَ يٰقَوْمِ اعْبُدُوا اللّٰهَ مَا لَكُمْ مِّنْ اِلٰهٍ غَيْرُهٗ ؕ اَفَلَا تَتَّقُوْنَ ﴿٦٦﴾

66. Na kwa Waadi (Tulimtuma) ndugu yao Hud. Akasema: Enyi kaumu yangu, Mwabuduni Allah, ninyi hamna mungu ghairi Yake; basi je, hamuogopi?

قَالَ الْمَلَاُ الَّذِيْنَ كَفَرُوْا مِنْ قَوْمِهٖٓ اِنَّا لَنَرٰىكَ فِيْ سَفَاهَةٍ وَّاِنَّا لَنَظُنُّكَ مِنَ الْكٰذِبِيْنَ ﴿٦٧﴾

67. Wakasema wakuu waliokufuru katika kaumu yake: Hakika sisi tunakuona umo katika upumbavu na kwa yakini tunakufahamu u miongoni mwa waongo.

Aya 65. *Watu vipofu,* yaani wasio na macho ya kiroho.

Aya 66. *'Aad* ni jina la kabila la watu wa zamani sana katika pande za bara Arabu. *Huud* ni jina la Mtume aliyetumwa kwa kabila la Waadi. Aliishi baada ya Nuhu na alikuwa wa saba kutoka kwake.

قَالَ يٰقَوْمِ لَيْسَ بِيْ سَفَاهَةٌ وَّلٰكِنِّيْ رَسُوْلٌ مِّنْ رَّبِّ الْعٰلَمِيْنَ ﴿٦٨﴾

68. Akasema: Enyi kaumu yangu, mimi sina upumbavu, bali mimi ni Mtume kutoka kwa Mola wa walimwengu.

اُبَلِّغُكُمْ رِسٰلٰتِ رَبِّيْ وَاَنَا لَكُمْ نَاصِحٌ اَمِيْنٌ ﴿٦٩﴾

69. Nawafikishieni risala za Mola wangu na mimi kwenu ni mtoa nasaha, mwaminifu.

اَوَعَجِبْتُمْ اَنْ جَآءَكُمْ ذِكْرٌ مِّنْ رَّبِّكُمْ عَلٰى رَجُلٍ مِّنْكُمْ لِيُنْذِرَكُمْ ؕ وَاذْكُرُوْٓا اِذْ جَعَلَكُمْ خُلَفَآءَ مِنْۢ بَعْدِ قَوْمِ نُوْحٍ وَّزَادَكُمْ فِي الْخَلْقِ بَصْۜطَةً ۚ فَاذْكُرُوْٓا اٰلَآءَ اللّٰهِ لَعَلَّكُمْ تُفْلِحُوْنَ ﴿٧٠﴾

70. Je, mnaona ajabu kuwafikieni mawaidha kutoka kwa Mola wenu kwa njia ya mtu aliye mmoja wenu ili awaonyeni? Na kumbukeni Alipowafanyeni makhalifa baada ya watu wa Nuhu na Amewazidishieni nguvu katika umbo. Basi mzikumbuke neema za Allah ili mpate kufaulu.

قَالُوْٓا اَجِئْتَنَا لِنَعْبُدَ اللّٰهَ وَحْدَهٗ وَنَذَرَ مَا كَانَ يَعْبُدُ اٰبَآؤُنَا ۚ فَاْتِنَا بِمَا تَعِدُنَآ اِنْ كُنْتَ مِنَ الصّٰدِقِيْنَ ﴿٧١﴾

71. Wakasema: Je, umetufikia ili tumwabudu Allah pekee na tuyaache waliyokuwa wakiabudu baba zetu? Basi tuletee unayotuahidi ukiwa miongoni mwa wasemao kweli.

قَالَ قَدْ وَقَعَ عَلَيْكُمْ مِّنْ رَّبِّكُمْ رِجْسٌ وَّغَضَبٌ ؕ اَتُجَادِلُوْنَنِيْ فِيْٓ اَسْمَآءٍ سَمَّيْتُمُوْهَآ اَنْتُمْ وَاٰبَآؤُكُمْ مَّا نَزَّلَ اللّٰهُ بِهَا مِنْ سُلْطٰنٍ ؕ فَانْتَظِرُوْٓا اِنِّيْ مَعَكُمْ مِّنَ الْمُنْتَظِرِيْنَ ﴿٧٢﴾

72. Akasema: Bila shaka adhabu na ghadhabu vimewaangukieni kutoka kwa Mola wenu. Je, mnajadiliana nami katika majina mliyoyaita ninyi na baba zenu ambayo kwayo Allah Hakuteremsha dalili? Basi ngojeni, mimi pia ni pamoja nanyi katika wangojeao.

فَاَنْجَيْنٰهُ وَالَّذِيْنَ مَعَهٗ بِرَحْمَةٍ مِّنَّا وَقَطَعْنَا دَابِرَ الَّذِيْنَ كَذَّبُوْا بِاٰيٰتِنَا وَمَا كَانُوْا مُؤْمِنِيْنَ ﴿٧٣﴾ ع

73. Basi Tukamuokoa yeye na waliokuwa pamoja naye kwa rehema Yetu, na Tukaukata mzizi wa wale waliozikadhibisha Aya Zetu na hawakuwa wenye kuamini.

Kabila la Waadi lilipata kutawala sehemu zenye rutuba za nchi ya Bara Arabu, hasa Yaman, Sham na Mesopotamia. Walikuwa ni watu wa kwanza kuitawala Bara Arabu yote. Walikuwa wakiitwa '*Aadanil'uulaa* yaani Waadi wa zamani.

Aya 72. Aya hii inaonyesha ya kuwa mtu anaweza kuwafuata baba zake ikiwa akili inakubali. Lakini kufuata tu kama kipofu kunalaumiwa.

FUNGU 10

وَاِلٰى ثَمُوْدَ اَخَاهُمْ صٰلِحًا ۘ قَالَ يٰقَوْمِ اعْبُدُوا اللّٰهَ مَا لَكُمْ مِّنْ اِلٰهٍ غَيْرُهٗ ؕ قَدْ جَآءَتْكُمْ بَيِّنَةٌ مِّنْ رَّبِّكُمْ ؕ هٰذِهٖ نَاقَةُ اللّٰهِ لَكُمْ اٰيَةً فَذَرُوْهَا تَاْكُلْ فِيْٓ اَرْضِ اللّٰهِ وَلَا تَمَسُّوْهَا بِسُوْٓءٍ فَيَاْخُذَكُمْ عَذَابٌ اَلِيْمٌ ﴿٧٣﴾

74. Na kwa Wathamudi (Tukamtuma) ndugu yao Saleh. Akasema: Enyi watu wangu, Mwabuduni Allah. Ninyi hamna mungu ila Yeye; hakika imekwisha wafikieni Ishara dhahiri kutoka kwa Mola wenu. Huyu ni ngamia jike wa Allah aliye ni Ishara kwenu. Basi mwacheni ale katika ardhi ya Mungu, wala msimtie dhara, isije ikawashikeni adhabu iumizayo.

وَاذْكُرُوْٓا اِذْ جَعَلَكُمْ خُلَفَآءَ مِنْۢ بَعْدِ عَادٍ وَّبَوَّاَكُمْ فِى الْاَرْضِ تَتَّخِذُوْنَ مِنْ سُهُوْلِهَا قُصُوْرًا وَّتَنْحِتُوْنَ الْجِبَالَ بُيُوْتًا ۚ فَاذْكُرُوْٓا اٰلَآءَ اللّٰهِ وَلَا تَعْثَوْا فِى الْاَرْضِ مُفْسِدِيْنَ ﴿٧٤﴾

75. Na kumbukeni Alipowafanyeni makhalifa baada ya Waadi na kuwakalisheni katika ardhi mkajenga ngome katika nyanda zake na mkachonga majumba katika majabali. Basi zikumbukeni neema za Allah, wala msiasi ardhini kwa kufanya uharibifu.

قَالَ الْمَلَاُ الَّذِيْنَ اسْتَكْبَرُوْا مِنْ قَوْمِهٖ لِلَّذِيْنَ اسْتُضْعِفُوْا لِمَنْ اٰمَنَ مِنْهُمْ اَتَعْلَمُوْنَ اَنَّ صٰلِحًا مُّرْسَلٌ مِّنْ رَّبِّهٖ ؕ قَالُوْٓا اِنَّا بِمَآ اُرْسِلَ بِهٖ مُؤْمِنُوْنَ ﴿٧٥﴾

76. Wakasema wakuu wa kaumu yake waliotakabari, kuwaambia wale walio dhaifu walioamini miongoni mwao: Je, mnajua ya kwamba Saleh Ametumwa na Mola wake? Wakasema: Hakika tunayaamini yale aliyotumwa nayo.

قَالَ الَّذِيْنَ اسْتَكْبَرُوْٓا اِنَّا بِالَّذِيْٓ اٰمَنْتُمْ بِهٖ كٰفِرُوْنَ ﴿٧٦﴾

77. Wakasema wale waliotakabari: Hakika sisi tunayakataa yale mnayoyaamini.

Aya 74. *Wathamudi* ni jina la kabila lililoishi baada ya Waadi. Kabila hili lilikaa sehemu za magharibi ya Bara Arabu na likaenea toka Aden upande wa kaskazini mpaka Sham. Kabila hili lilikuwepo mara baada ya Nabii Ismail. Nchi yao ilikuwa karibu na nchi ya Waadi, lakini wao zaidi walikaa vilimani.

Huyu ni ngamia jike wa Allah. Ngamia ndiye mnyama anayesafiriwa sana katika Bara Arabu; na Nabii Saleh alikuwa akisafiri kwenda huko na huko kuhubiri juu ya huyo ngamia wake. Basi aliwaambia watu wake ya kuwa kumzuia ngamia wake ni kama kuzuia kazi ya Allah anayoifanya. Hivyo ngamia yule akafanywa kuwa Ishara kwa ajili ya watu wale, naye alikuwa ni mnyama tu kama ngamia wengine.

فَعَقَرُوا النَّاقَةَ وَعَتَوْا عَنْ اَمْرِ رَبِّهِمْ وَقَالُوْا يٰصٰلِحُ ائْتِنَا بِمَا تَعِدُنَآ اِنْ كُنْتَ مِنَ الْمُرْسَلِيْنَ ﴿٧٨﴾

78. Na wakaikata miguu ya ngamia yule na kuasi amri ya Mola wao na wakasema: Ee Saleh, tuletee unayotuahidi ikiwa wewe u miongoni mwa Mitume.

فَاَخَذَتْهُمُ الرَّجْفَةُ فَاَصْبَحُوْا فِيْ دَارِهِمْ جٰثِمِيْنَ ﴿٧٩﴾

79. Ndipo likawashika tetemeko la ardhi na wakawa wenye kuanguka kifudifudi majumbani mwao.

فَتَوَلّٰى عَنْهُمْ وَقَالَ يٰقَوْمِ لَقَدْ اَبْلَغْتُكُمْ رِسَالَةَ رَبِّيْ وَنَصَحْتُ لَكُمْ وَلٰكِنْ لَّا تُحِبُّوْنَ النّٰصِحِيْنَ ﴿٨٠﴾

80. Basi (Saleh) akawaacha na akasema: Enyi kaumu yangu, kwa yakini nimewafikishieni ujumbe wa Mola wangu na nimewasihini, lakini ninyi hamwapendi watoao nasaha.

وَلُوْطًا اِذْ قَالَ لِقَوْمِهٖٓ اَتَاْتُوْنَ الْفَاحِشَةَ مَا سَبَقَكُمْ بِهَا مِنْ اَحَدٍ مِّنَ الْعٰلَمِيْنَ ﴿٨١﴾

81. Na (Tulimtuma) Luti alipowaambia kaumu yake: Je, mnafanya ufasiki ambao hajawatangulieni ye yote kwa huo katika walimwengu?

اِنَّكُمْ لَتَاْتُوْنَ الرِّجَالَ شَهْوَةً مِّنْ دُوْنِ النِّسَآءِ ؕ بَلْ اَنْتُمْ قَوْمٌ مُّسْرِفُوْنَ ﴿٨٢﴾

82. Hakika ninyi mnafika kwa wanaume kwa kuwaingilia badala ya wanawake, bali ninyi ni watu warukao mipaka!

وَمَا كَانَ جَوَابَ قَوْمِهٖٓ اِلَّآ اَنْ قَالُوْٓا اَخْرِجُوْهُمْ مِّنْ قَرْيَتِكُمْ ۚ اِنَّهُمْ اُنَاسٌ يَّتَطَهَّرُوْنَ ﴿٨٣﴾

83. Na hayakuwa majibu ya kaumu yake isipokuwa wakasema: Wafukuzeni katika mji wenu, maana hao ni watu wanaojifanya wametakasika.

فَاَنْجَيْنٰهُ وَاَهْلَهٗٓ اِلَّا امْرَاَتَهٗ ۖ كَانَتْ مِنَ الْغٰبِرِيْنَ ﴿٨٤﴾

84. Basi Tukamuokoa yeye na watu wa nyumbani mwake isipokuwa mke wake, alikuwa miongoni mwa wakaao nyuma.

وَاَمْطَرْنَا عَلَيْهِمْ مَّطَرًا ؕ فَانْظُرْ كَيْفَ كَانَ عَاقِبَةُ الْمُجْرِمِيْنَ ﴿٨٥﴾ ع ١٢ ١٧

85. Na Tukawanyeshea mvua (ya adhabu). Basi tazama jinsi ulivyokuwa mwisho wa wakosefu.

Aya 79. *Bila ya kujimudu.* Neno lililotumiwa katika Kiarabu ni *Jaathimiin* ambalo maana yake ni: (1) Tetemeko liliwaua kwa kuwaponda na *wakalala kifudifudi;* (2) Tetemeko lilipowashika walitishika wakaanguka *kifudifudi* wakiomba Mungu awaponyeshe.

Aya 81. *Luut* alikuwa mtoto wa ndugu wa Ibrahimu, na wote wawili walikuwa katika wakati mmoja (Mwanzo 11:27, 31). Pia tazama sura 6:87.

Nabii Luti aliwakaripia watu wake si kwa uovu mkubwa mno wa kufirana tu, bali pia walizidi kiasi katika maovu mengine.

FUNGU 11

وَاِلٰى مَدْيَنَ اَخَاهُمْ شُعَيْبًا ؕ قَالَ يٰقَوْمِ اعْبُدُوا اللّٰهَ مَا لَكُمْ مِّنْ اِلٰهٍ غَيْرُهٗ ؕ قَدْ جَآءَتْكُمْ بَيِّنَةٌ مِّنْ رَّبِّكُمْ فَاَوْفُوا الْكَيْلَ وَالْمِيْزَانَ وَلَا تَبْخَسُوا النَّاسَ اَشْيَآءَهُمْ وَلَا تُفْسِدُوْا فِى الْاَرْضِ بَعْدَ اِصْلَاحِهَا ؕ ذٰلِكُمْ خَيْرٌ لَّكُمْ اِنْ كُنْتُمْ مُّؤْمِنِيْنَ ۚ﴿۸۶﴾

86. Na kwa Wamadiana (Tukamtuma) ndugu yao Shuaibu. Akasema: Enyi kaumu yangu, Mwabuduni Allah, hamna mungu ghairi yake. Hakika imekwisha wafikieni Ishara dhahiri kutoka kwa Mola wenu. Basi kamilisheni kipimo sawasawa na mizani (pia), wala msiwapunguzie watu (vipimo vya) vitu vyao, wala msifanye uharibifu katika ardhi ikiisha suluhika; hivi ndivyo bora kwenu ikiwa ninyi ni wenye kuamini.

وَلَا تَقْعُدُوْا بِكُلِّ صِرَاطٍ تُوْعِدُوْنَ وَتَصُدُّوْنَ عَنْ سَبِيْلِ اللّٰهِ مَنْ اٰمَنَ بِهٖ وَتَبْغُوْنَهَا عِوَجًا ۚ وَاذْكُرُوْٓا اِذْ كُنْتُمْ قَلِيْلًا فَكَثَّرَكُمْ ۪ وَانْظُرُوْا كَيْفَ كَانَ عَاقِبَةُ الْمُفْسِدِيْنَ ﴿۸۷﴾

87. Wala msikalie kila njia kumwogopesha na kumzuilia njia ya Allah mwenye kumwamini, na kutaka kuipotosha. Na kumbukeni mlipokuwa wachache naye Akawafanyeni kuwa wengi, na tazameni jinsi ulivyokuwa mwisho wa waharibifu.

وَاِنْ كَانَ طَآئِفَةٌ مِّنْكُمْ اٰمَنُوْا بِالَّذِىْٓ اُرْسِلْتُ بِهٖ وَطَآئِفَةٌ لَّمْ يُؤْمِنُوْا فَاصْبِرُوْا حَتّٰى يَحْكُمَ اللّٰهُ بَيْنَنَا ۚ وَهُوَ خَيْرُ الْحٰكِمِيْنَ ﴿۸۸﴾

88. Na kama liko taifa miongoni mwenu lililoamini yale niliyotumwa nayo na taifa jingine lisiloamini, basi subirini mpaka Allah Ahukumu kati yetu; naye ndiye Mbora wa mahakimu.

Aya 86. *Madyan* ni jina la mtoto wa Nabii Ibrahimu aliyezaliwa na Mkewe Katurah (Mwanzo 25:1,2). Wazao wa huyu Madiani walikaa kaskazini ya Hijaz. Kadhalika Madiani lilikuwa jina la mji karibu na bahari ya Sham mbele ya Sinai katika pwani ya Bara Arabu. Mji huu ulipewa jina hili kwa sababu ulikaliwa na wazao wa Madiani.

Shu'aib lilikuwa jina la Mtume asiyekuwa wa Kiisraeli aliyekuwako kabla ya Nabii Musa. Anafahamiwa kuwa mkwe wa Nabii Musa ingawa Biblia haitaji jina hili. Hadithi ya Biblia inasema ya kuwa mkwewe Nabii Musa alikuwa Jethro ambaye hatajwi kuwa Mtume.

Aya hi inaeleza ya kuwa uovu mkubwa wa watu wa Madiani ulikuwa ni kupunja katika vipimo na mizani.

JUZU 9

قَالَ الْمَلَاُ الَّذِيْنَ اسْتَكْبَرُوْا مِنْ ۛ قَوْمِهٖ لَنُخْرِجَنَّكَ يٰشُعَيْبُ وَالَّذِيْنَ اٰمَنُوْا مَعَكَ مِنْ قَرْيَتِنَآ اَوْ لَتَعُوْدُنَّ فِيْ مِلَّتِنَا ؕ قَالَ اَوَلَوْ كُنَّا كٰرِهِيْنَ ﴿۸۸﴾

89. Wakuu waliotakabari katika kaumu yake wakasema: Ewe Shuaibu, kwa yakini tutakutoa wewe na wale walioamini pamoja nawe katika mji wetu, au hamna budi kurudi katika mila yetu. Akasema: Je, ingawa tunaichukia?

قَدِ افْتَرَيْنَا عَلَى اللّٰهِ كَذِبًا اِنْ عُدْنَا فِيْ مِلَّتِكُمْ بَعْدَ اِذْ نَجّٰىنَا اللّٰهُ مِنْهَا ؕ وَمَا يَكُوْنُ لَنَآ اَنْ نَّعُوْدَ فِيْهَآ اِلَّآ اَنْ يَّشَآءَ اللّٰهُ رَبُّنَا ؕ وَسِعَ رَبُّنَا كُلَّ شَيْءٍ عِلْمًا ؕ عَلَى اللّٰهِ تَوَكَّلْنَا ؕ رَبَّنَا افْتَحْ بَيْنَنَا وَبَيْنَ قَوْمِنَا بِالْحَقِّ وَاَنْتَ خَيْرُ الْفٰتِحِيْنَ ﴿۸۹﴾

90. Bila shaka tumemtungia Allah uwongo ikiwa tutarudi katika mila yenu baada ya kutuokoa Allah katika hiyo; wala hatuwezi kuirudia mpaka Apende Allah, Mola wetu. Katika elimu Mola wetu Anatambua kila kitu. Juu ya Allah tunategemea. Mola wetu! hukumu baina yetu na baina ya kaumu yetu kwa haki, nawe ndiwe Mbora wa wanaohukumu.

وَقَالَ الْمَلَاُ الَّذِيْنَ كَفَرُوْا مِنْ قَوْمِهٖ لَئِنِ اتَّبَعْتُمْ شُعَيْبًا اِنَّكُمْ اِذًا لَّخٰسِرُوْنَ ﴿۹۰﴾

91. Na wakuu waliokufuru katika kaumu yake wakasema: Kama ninyi mkimfuata Shuaibu, hapo bila shaka mtakuwa wenye hasara.

فَاَخَذَتْهُمُ الرَّجْفَةُ فَاَصْبَحُوْا فِيْ دَارِهِمْ جٰثِمِيْنَ ﴿۹۱﴾

92. Basi likawashika tetemeko la nchi na wakawa wasiojimudu majumbani mwao.

الَّذِيْنَ كَذَّبُوْا شُعَيْبًا كَاَنْ لَّمْ يَغْنَوْا فِيْهَا ۚ اَلَّذِيْنَ كَذَّبُوْا شُعَيْبًا كَانُوْا هُمُ الْخٰسِرِيْنَ ﴿۹۲﴾

93. Wale waliomkadhibisha Shuaibu wakawa kana kwamba hawakuwamo. Wale waliomkadhibisha Shuaibu walikuwa ndio wenye hasara.

فَتَوَلّٰى عَنْهُمْ وَقَالَ يٰقَوْمِ لَقَدْ اَبْلَغْتُكُمْ رِسٰلٰتِ رَبِّيْ وَنَصَحْتُ لَكُمْ ۚ فَكَيْفَ اٰسٰى عَلٰى قَوْمٍ كٰفِرِيْنَ ﴿۹۳﴾

94. Basi akawaachilia mbali na akasema: Enyi kaumu yangu, bila shaka nimewafikishieni risala za Mola wangu na nimewasihini; basi nihuzunikeje juu ya watu makafiri?

Aya 92. Watu wa Nabii Shuaibu waliangamizwa kwa adhabu ya zilzala (tetemeko la nchi) yumkini wakati wa asubuhi.

FUNGU 12

وَمَآ اَرْسَلْنَا فِيْ قَرْيَةٍ مِّنْ نَّبِيٍّ اِلَّآ اَخَذْنَآ اَهْلَهَا بِالْبَاْسَآءِ وَالضَّرَّآءِ لَعَلَّهُمْ يَضَّرَّعُوْنَ ﴿٩٥﴾

95. Na Hatukumtuma Nabii ye yote katika mji wo wote isipokuwa Tuliwashika wenyeji wake kwa taabu na mashaka ili wapate kunyenyekea.

ثُمَّ بَدَّلْنَا مَكَانَ السَّيِّئَةِ الْحَسَنَةَ حَتّٰى عَفَوْا وَّقَالُوْا قَدْ مَسَّ اٰبَآءَنَا الضَّرَّآءُ وَالسَّرَّآءُ فَاَخَذْنٰهُمْ بَغْتَةً وَّهُمْ لَا يَشْعُرُوْنَ ﴿٩٦﴾

96. Kisha Tukabadilisha mahali pa ubaya kwa wema, hata wakazidi (kuneemeka na kuwa wengi) na wakasema: (Zamani) taabu na raha ziliwafikia baba zetu. Basi Tuliwashika kwa ghafla hali hawatambui.

وَلَوْ اَنَّ اَهْلَ الْقُرٰٓى اٰمَنُوْا وَاتَّقَوْا لَفَتَحْنَا عَلَيْهِمْ بَرَكٰتٍ مِّنَ السَّمَآءِ وَالْاَرْضِ وَلٰكِنْ كَذَّبُوْا فَاَخَذْنٰهُمْ بِمَا كَانُوْا يَكْسِبُوْنَ ﴿٩٧﴾

97. Na lau kama watu wa mji wangaliamini na kuogopa, kwa yakini Tungaliwafungulia baraka za mbingu na ardhi; lakini walikadhibisha, kwa hiyo Tukawashika kwa sababu ya yale waliyokuwa wakiyachuma.

اَفَاَمِنَ اَهْلُ الْقُرٰٓى اَنْ يَّاْتِيَهُمْ بَاْسُنَا بَيَاتًا وَّهُمْ نَآئِمُوْنَ ﴿٩٨﴾

98. Je watu wa miji wamesalimika ya kuwa adhabu Yetu haitawafikia usiku hali wamelala?

اَوَاَمِنَ اَهْلُ الْقُرٰٓى اَنْ يَّاْتِيَهُمْ بَاْسُنَا ضُحًى وَّهُمْ يَلْعَبُوْنَ ﴿٩٩﴾

99. Au watu wa miji wamesalimika ya kuwa adhabu yetu haitawafikia mchana hali wakicheza?

اَفَاَمِنُوْا مَكْرَ اللّٰهِ ۚ فَلَا يَاْمَنُ مَكْرَ اللّٰهِ اِلَّا الْقَوْمُ الْخٰسِرُوْنَ ﴿١٠٠﴾

100. Je, wako salama katika mipango ya Allah? Lakini hapana anayedhani kuwa yu salama katika mipango ya Allah ila watu wenye hasara.

Aya 95. Mambo mawili yanaonekana katika Aya hii: (1) Misiba yenye kuenea kote-kote haiwafikii watu mpaka Nabii wa Munguametumwa; (2) ni jambo lisilotokea kuwa kufika kwa Nabii wa Mungu kusifuatane na misiba iliyozagaa.

Aya 98. Katika Aya hii na ifuatayo, maneno, *watu wa miji*, yanawahusu watu wa siku za Mtume *s.a.w.* ambao sasa Qur'an inawageukia baada ya kutaja watu wa zamani walioangamizwa kwa kukataa Manabii wao. Aya hii inataka kuwaonya watu wa Makka na miji mingine ya Bara Arabu ya kwamba zamu yao inawasogelea, na ya kwamba adhabu ya Allah inaweza kuwafikia wakati wo wote wa kutojali kwao.

FUNGU 13

اَوَلَمْ يَهْدِ لِلَّذِيْنَ يَرِثُوْنَ الْاَرْضَ مِنْۢ بَعْدِ اَهْلِهَآ اَنْ لَّوْ نَشَآءُ اَصَبْنٰهُمْ بِذُنُوْبِهِمْ ۚ وَنَطْبَعُ عَلٰى قُلُوْبِهِمْ فَهُمْ لَا يَسْمَعُوْنَ ﴿١٠١﴾

101. Je! haiwaongozi wale wanaoirithi ardhi baada ya wenyeji wake kwamba Tukitaka Tunaweza kuwatia msiba kwa dhambi zao na Kupiga muhuri juu ya mioyo yao kwa hiyo hawatasikia?

تِلْكَ الْقُرٰى نَقُصُّ عَلَيْكَ مِنْ اَنْۢبَآئِهَا ۚ وَلَقَدْ جَآءَتْهُمْ رُسُلُهُمْ بِالْبَيِّنٰتِ ۚ فَمَا كَانُوْا لِيُؤْمِنُوْا بِمَا كَذَّبُوْا مِنْ قَبْلُ ؕ كَذٰلِكَ يَطْبَعُ اللّٰهُ عَلٰى قُلُوْبِ الْكٰفِرِيْنَ ﴿١٠٢﴾

102. Hiyo ni miji tunakusimulia baadhi ya habari zao, na bila shaka Mitume wao waliwafikia kwa Ishara waziwazi, lakini hawakuwa wenye kuamini waliyoyakadhibisha zamani. Hivi ndivyo Allah Apigavyo muhuri mioyo ya makafiri.

وَمَا وَجَدْنَا لِاَكْثَرِهِمْ مِّنْ عَهْدٍ ۚ وَاِنْ وَّجَدْنَآ اَكْثَرَهُمْ لَفٰسِقِيْنَ ﴿١٠٣﴾

103. Na kwa wengi wao Hatukukuta staha yo yote ya kutimiza ahadi bali kwa hakika wengi wao Tuliwakuta waasi tu.

ثُمَّ بَعَثْنَا مِنْۢ بَعْدِهِمْ مُّوْسٰى بِاٰيٰتِنَآ اِلٰى فِرْعَوْنَ وَمَلَا۟ئِهٖ فَظَلَمُوْا بِهَا ۚ فَانْظُرْ كَيْفَ كَانَ عَاقِبَةُ الْمُفْسِدِيْنَ ﴿١٠٤﴾

104. Kisha baada yao Tukamtuma Musa na Ishara Zetu kwa Firauni na wakuu wake. Lakini walizikataa kwa dhulma; basi tazama jinsi ulivyokuwa mwisho wa waharibifu.

وَقَالَ مُوْسٰى يٰفِرْعَوْنُ اِنِّيْ رَسُوْلٌ مِّنْ رَّبِّ الْعٰلَمِيْنَ ﴿١٠٥﴾ۙ

105. Na akasema Musa: Ewe Firauni, kwa hakika mimi ni Mtume nitokaye kwa Mola wa walimwengu,

حَقِيْقٌ عَلٰٓى اَنْ لَّآ اَقُوْلَ عَلَى اللّٰهِ اِلَّا الْحَقَّ ؕ قَدْ جِئْتُكُمْ بِبَيِّنَةٍ مِّنْ رَّبِّكُمْ فَاَرْسِلْ مَعِيَ بَنِيْٓ اِسْرَآءِيْلَ ﴿١٠٦﴾ؕ

106. Yanipasa nisiseme juu ya Allah isipokuwa haki. Kwa yakini nimewafikieni kwa dalili wazi itokayo kwa Mola wenu, basi wapeleke wana wa Israeli pamoja nami

قَالَ اِنْ كُنْتَ جِئْتَ بِاٰيَةٍ فَاْتِ بِهَآ اِنْ كُنْتَ مِنَ الصّٰدِقِيْنَ ﴿١٠٧﴾

107. (Firauni) akasema: Kama umekuja na Ishara, basi ilete ikiwa u miongoni mwa wasemao kweli.

Aya 102. Neno *alquraa* (miji) hapa linahusu miji ya zamani iliyoangamizwa. Qur'an inarejea kuitaja ili kutia mkazo jinsi lilivyo jambo la hatari kumkataa Nabii;na pia inawaambia habari ya watu wengine wa zamani waliomkataa Musa. Aya hii inadokeza ya kwamba kwa kuwa Mtume *s.a.w.* ni badala ya Manabii wote waliomtangulia, basi wanaomkataa watapata kila namna ya adhabu zilizowafikia watu waliowakataa Manabii wa zamani.

108. Ndipo akaitupa fimbo yake فَاَلْقٰى عَصَاهُ فَاِذَا هِىَ ثُعْبَانٌ مُّبِيْنٌ ۚ﴿١٠٨﴾
mara ikawa nyoka dhahiri.

109. Na akatoa mkono wake, mara وَّنَزَعَ يَدَهٗ فَاِذَا هِىَ بَيْضَآءُ لِلنّٰظِرِيْنَ ﴿١٠٩﴾
ukawa mweupe kwa watazamao.

Aya 108. Qur'an imeumia maneno ya namna tatu kwa kueleza kugeuka nyoka kwa fimbo ya Nabii Musa: (1) *Thu'baan,* kama lilivyo katika Aya hii na katika sura 26:33; (2) *Hayyatun,* kama lilivyo katika sura 20:21; na (3) *Jaannu*, kama lilivyo katika sura 28:32 na 27:11. Neno *Thu'baan* na *Hayyatun* hutumika kwa nyoka mkubwa na mdogo; ambapo neno *Jaannu* linaonyesha nyoka mdogo tu. Hivyo, hakuna matatanisho katika kutumia maneno haya matatu, kwa vile yote yanatoa maana moja.

Fimbo ile ilionekana kama nyoka aendaye. Ilikuwa ni namna ya mwujiza unaoonyeshwa kwa njozi, ambao Allah aliufanya kwa kuyafanya macho ya watazamaji waione fimbo katika umbo la nyoka; na njozi ilionwa na Firauni, na mawaziri wake, na wachawi, na Musa kadhalika.

Jambo kama hili lilitokea wakati wa Mtume s.a.w. mwezi ulipoonekana umepasuka; na si kama aliona Mtume tu, bali pia wafuasi wake na maadui zake (Bukhari, sura *Tafsiir*).

MALAIKA WALIONEKANA.

Kadhalika Hadithi zinatusimulia ya kuwa Malaika Jibrili, ambaye Mtume *s.a.w* alikuwa akimwona mara kwa mara katika njozi, masahaba waliokuwa wanaketi pamoja naye walipata mara moja kumwona (Bukhari, sura *Imaan*). Tena, baadhi ya Malaika walionwa hata na wasioamini siku ya vita vya Badri (Jarir, jalada 6, uk. 47).

NJOZI YA SEYYIDNA UMAR.

Jambo jingine la namna hii lilitokea wakati jeshi la Waislamu, lililokuwa linaongozwa na Amiri maarufu wa Kiislamu aitwaye Sariya, lilipokuwa linapigana na adui katika Irak, umbali wa maili mamia na mamia kutoka Madina. Seyidna Umar, Khalifa wa Pili, alipokuwa akitoa hotuba ya Sala ya Ijumaa, akaona katika njozi ya kuwa jeshi la Waislamu linahemewa na wingi mkubwa wa maadui, na karibu kabisa kushindwa. Mara moja Seyidna Umar akaacha kutoa hotuba na akapiga kelele juu ya mimbar, Ee Sariya: nenda kwenye mlima, nenda kwenye mlima." Sariya, kule aliko, hali amezungukwa na kelele za panga, akaisikia sauti ile ya Sayidna Umar na akaenda kwenye mlima na jeshi la Waislamu likasalimika (Khamis jalada 2 uk. 270).

MWUJIZA WA MTUME.

Abu Jahal, aliyekuwa adui mkubwa wa Mtume *s.a.w*. alipata naye kuona njozi ya namna hii. Abu Jahal alikuwa anadaiwa na mtu mmoja mgeni, aliyefika Makka, pesa ambazo hakutaka kuzilipa. Mtu yule akafika kwa Mtume *s.a.w.* kushtakia alivyodhulumiwa. Mtume *s.a.w.* aliondoka akafika kwa Abu Jahal kuzidai pesa zile; na Abu Jahal akazilipa pale pale kwa haraka . Alipoulizwa Abu Jahal kwa nini amefanya woga na kuzilipa pesa zile. Akasema ya kuwa aliona ngamia wawili wenye hasira upande wa kushoto na wa kulia wa Muhammad, walio tayari kumrarua kama hakulipa (Hisham). Bara Arabu ni nchi ya ngamia, hivyo Abu Jahal akaonyeshwa ngamia. Lakini Misri ni nchi ya nyoka za uchawi, basi Firauni akaonyeshwa nyoka.

FUNGU 14

قَالَ الْمَلَاُ مِنْ قَوْمِ فِرْعَوْنَ اِنَّ هٰذَا لَسٰحِرٌ عَلِيْمٌ ﴿١١٠﴾

110. Wakasema wakuu wa kaumu ya Firauni Hakika huyu ni mchawi ajuaye.

يُّرِيْدُ اَنْ يُّخْرِجَكُمْ مِّنْ اَرْضِكُمْ ۚ فَمَاذَا تَاْمُرُوْنَ ﴿١١١﴾

111. Anataka kuwatoeni katika ardhi yenu. Basi mnatoa shauri gani?

قَالُوْٓا اَرْجِهْ وَاَخَاهُ وَاَرْسِلْ فِى الْمَدَآئِنِ حٰشِرِيْنَ ﴿١١٢﴾

112. Wakasema mwache kidogo yeye na ndugu yake, na uwatume waku sanyao katika miji.

يَاْتُوْكَ بِكُلِّ سَحَّارٍ عَلِيْمٍ ﴿١١٣﴾

113. Wakuletee kila mchawi ajuaye

وَجَآءَ السَّحَرَةُ فِرْعَوْنَ قَالُوْٓا اِنَّ لَنَا لَاَجْرًا اِنْ كُنَّا نَحْنُ الْغٰلِبِيْنَ ﴿١١٤﴾

114. Na wakaja wachawi kwa Firauni, wakasema: Hakika tutapata ujira ikiwa tutashinda?

قَالَ نَعَمْ وَاِنَّكُمْ لَمِنَ الْمُقَرَّبِيْنَ ﴿١١٥﴾

115. Akasema: Naam, nanyi bila shaka mtakuwa miongoni mwa walio karibu (nami).

قَالُوْا يٰمُوْسٰٓى اِمَّآ اَنْ تُلْقِىَ وَاِمَّآ اَنْ نَّكُوْنَ نَحْنُ الْمُلْقِيْنَ ﴿١١٦﴾

116. Wakasema: Ewe Musa, je, utatupa wewe au tutakuwa sisi watupao (kwanza)?

قَالَ اَلْقُوْا ۚ فَلَمَّآ اَلْقَوْا سَحَرُوْٓا اَعْيُنَ النَّاسِ وَاسْتَرْهَبُوْهُمْ وَجَآءُوْ بِسِحْرٍ عَظِيْمٍ ﴿١١٧﴾

117. Akasema: Tupeni. Basi wali potupa wakayaghilibu macho ya watu,na wakawaogopesha, na wakaleta uchawi mkubwa.

وَاَوْحَيْنَآ اِلٰى مُوْسٰٓى اَنْ اَلْقِ عَصَاكَ ۚ فَاِذَا هِىَ تَلْقَفُ مَا يَاْفِكُوْنَ ﴿١١٨﴾ ۚ

118. Na Tukamfunulia Musa ya kwamba, tupa fimbo yako. Mara ikavimeza walivyovizua.

فَوَقَعَ الْحَقُّ وَبَطَلَ مَا كَانُوْا يَعْمَلُوْنَ ﴿١١٩﴾ ۚ

119. Basi haki ikadhihiri na yakabatilika waliyokuwa wakiyatenda.

فَغُلِبُوْا هُنَالِكَ وَانْقَلَبُوْا صٰغِرِيْنَ ﴿١٢٠﴾ ۚ

120. Kwa hiyo walishindwa pale pale, na wakarudi wamedhalilika.

Aya 110. *Saahir,* "Mchawi" Neno hili si kwamba lazima liwe kila mara kwa maana ya mchawi. Pia lina maana ya mlozi; mtu anayeliwaza na kutumbuiza; mtu anayejua, stadi na mwenye akili; mtu mwenye uwezo kukifanya kitu kionekane namna nyingine kuliko hasa kilivyo; mdanganyaji, mlaghai n.k.w. (Akrab na Lane).

Aya 117. Nabii Musa alikuwa mwepesi kushika nafasi aliyopewa na akawajibu, watupe wao kwanza. Kwa desturi, Manabii wa Mungu hungoja waanzwe na maadui zao, kisha wao hujikinga na kungoja msaada wa Allah.

وَاُلْقِيَ السَّحَرَةُ سُجِدِيْنَ ﴿١٢٠﴾

121. Na wachawi wakaangushwa kusujudu.

قَالُوْٓا اٰمَنَّا بِرَبِّ الْعٰلَمِيْنَ ﴿١٢٢﴾

122. Wakasema: Tumemwamini Mola wa walimwengu.

رَبِّ مُوْسٰى وَهٰرُوْنَ ﴿١٢٣﴾

123. Mola wa Musa na Harun.

قَالَ فِرْعَوْنُ اٰمَنْتُمْ بِهٖ قَبْلَ اَنْ اٰذَنَ لَكُمْ ۚ اِنَّ هٰذَا لَمَكْرٌ مَّكَرْتُمُوْهُ فِي الْمَدِيْنَةِ لِتُخْرِجُوْا مِنْهَآ اَهْلَهَا ۚ فَسَوْفَ تَعْلَمُوْنَ ﴿١٢٤﴾

124. Akasema Firauni: Je, mmemwamini kabla sijawaruhusuni? Kwa yakini hii ndio hila mliyoifanya mjini ili muwatoe humo wenyeji wake. Lakini hivi karibuni mtajua.

لَاُقَطِّعَنَّ اَيْدِيَكُمْ وَاَرْجُلَكُمْ مِّنْ خِلَافٍ ثُمَّ لَاُصَلِّبَنَّكُمْ اَجْمَعِيْنَ ﴿١٢٥﴾

125. Lazima nitaikata mikono yenu na miguu yenu kwa upande tofauti, kisha nitawasulubuni ninyi nyote.

قَالُوْٓا اِنَّآ اِلٰى رَبِّنَا مُنْقَلِبُوْنَ ﴿١٢٦﴾ ۚ

126. Wakasema: Hakika sisi ni wenye kurudi kwa Mola wetu.

وَمَا تَنْقِمُ مِنَّآ اِلَّآ اَنْ اٰمَنَّا بِاٰيٰتِ رَبِّنَا لَمَّا جَآءَتْنَا ۭ رَبَّنَآ اَفْرِغْ عَلَيْنَا صَبْرًا وَّتَوَفَّنَا مُسْلِمِيْنَ ﴿١٢٧﴾ ع

127. Nawe hutufanyii kisasi ila kwa sababu tumeziamini Ishara za Mola wetu zilipotufikia. Mola wetu, tumiminie uvumilivu na Utufishe watii.

FUNGU 15

وَقَالَ الْمَلَاُ مِنْ قَوْمِ فِرْعَوْنَ اَتَذَرُ مُوْسٰى وَقَوْمَهٗ لِيُفْسِدُوْا فِي الْاَرْضِ وَيَذَرَكَ وَاٰلِهَتَكَ ۭ قَالَ سَنُقَتِّلُ اَبْنَآءَهُمْ وَنَسْتَحْيٖ نِسَآءَهُمْ ۚ وَاِنَّا فَوْقَهُمْ قٰهِرُوْنَ ﴿١٢٨﴾

128. Na wakasema wakuu wa kaumu ya Firauni: Je, utamuacha Musa na watu wake walete uharibifu katika nchi na kukuacha wewe na miungu wako? Akasema: Hivi karibuni tutawaua wavulana wao na kuwaacha hai wanawake wao, na bila shaka sisi ni wenye nguvu juu yao.

Aya 121. *Wakaangushwa kusujudu*. Kushindwa kwao kuliwavunja nguvu kabisa, wakaanguka kusujudu wakimnyenyekea Mungu.

Aya 124. *Hii ndio hila mliyoifanya.* Kupinduka kwa ghafla kwa hawa wachawi, kwa uwezo huu wa Allah, kukamfanya Firauni aanze kuwashuku wachawi; au tuseme, alisema maneno haya ili kuficha fedheha aliyoipata.

Biblia pia inakubaliana na Qur'an kwa kusema kuwa wale wachawi walimwamini Musa (Kutoka 8:19). Tofauti hapa ni kuwa Qur'an inasema, wale wachawi waliamini wakati ule ule walipoona mwujiza: ambapo Biblia inasema, waliamini baadaye. Maelezo ya Qur'an ndio yanaelekea kuwa sahihi zaidi.

قَالَ مُوْسٰى لِقَوْمِهِ اسْتَعِيْنُوْا بِاللّٰهِ
وَاصْبِرُوْا ۚ اِنَّ الْاَرْضَ لِلّٰهِ ۙ يُوْرِثُهَا
مَنْ يَّشَآءُ مِنْ عِبَادِهٖ ؕ وَالْعَاقِبَةُ
لِلْمُتَّقِيْنَ ﴿١٢٩﴾

129. Musa akawaambia kaumu yake: Ombeni msaada kwa Allah na subirini. Hakika ardhi ni ya Allah, Atairithisha Amtakaye katika watumishi Wake; na mwisho (mwema) ni kwa wamchao.

قَالُوْٓا اُوْذِيْنَا مِنْ قَبْلِ اَنْ تَاْتِيَنَا وَمِنْۢ بَعْدِ
مَا جِئْتَنَا ؕ قَالَ عَسٰى رَبُّكُمْ اَنْ يُّهْلِكَ
عَدُوَّكُمْ وَيَسْتَخْلِفَكُمْ فِى الْاَرْضِ
فَيَنْظُرَ كَيْفَ تَعْمَلُوْنَ ﴿١٣٠﴾ ع

130. Wakasema: Tumeudhiwa kabla hujatufikia na pia baada ya wewe kutujia. (Musa) akasema: Huenda Mola wenu Atamwangamiza adui yenu na kuwafanyeni makhalifa katika nchi,na Aone jinsi mtakavyofanya.

FUNGU 16

وَلَقَدْ اَخَذْنَآ اٰلَ فِرْعَوْنَ بِالسِّنِيْنَ
وَنَقْصٍ مِّنَ الثَّمَرٰتِ لَعَلَّهُمْ
يَذَّكَّرُوْنَ ﴿١٣١﴾

131. Na hakika tuliwaadhibu watu wa Firauni kwa njaa na upungufu wa matunda, ili wapate kushika nasaha.

فَاِذَا جَآءَتْهُمُ الْحَسَنَةُ قَالُوْا لَنَا هٰذِهٖ ۚ
وَاِنْ تُصِبْهُمْ سَيِّئَةٌ يَّطَّيَّرُوْا بِمُوْسٰى
وَمَنْ مَّعَهٗ ؕ اَلَآ اِنَّمَا طٰٓئِرُهُمْ عِنْدَ اللّٰهِ
وَلٰكِنَّ اَكْثَرَهُمْ لَا يَعْلَمُوْنَ ﴿١٣٢﴾

132. Bali ulipowafikia wema, wakasema: Huu ni kwa ajili yetu. Na ukiwafikia ubaya husema: Ni mkosi kwa ajili ya Musa na walio pamoja naye. Sikilizeni! hakika mkosi wao ni kwa Allah, lakini wengi wao hawajui.

وَقَالُوْا مَهْمَا تَاْتِنَا بِهٖ مِنْ اٰيَةٍ لِّتَسْحَرَنَا بِهَا ۙ
فَمَا نَحْنُ لَكَ بِمُؤْمِنِيْنَ ﴿١٣٣﴾

133. Na wakasema: Ishara yo yote utakayotuletea ili utuloge kwayo pia hatutakuamini.

Aya 129. Firauni alijivunia sana nguvu na mamlaka yake, na alikuwa mjeuri kupita kiasi; hivyo, Waisraeli wanaambiwa na Nabii Musa maneno ya kuwafariji na kuwatia moyo kuwa hawana haja ya kumwogopa Firauni, maana nguvu yake itavunjwa, na ufalme wake utatoka mikononi mwake.

Aya 131. Aya hii inataja adhabu namna mbili zilizowafikia watu wa Firauni - Kupotelewa na vitu, na vifo. Neno *thamaraat* lina maana ya matunda na watoto. Habari zaidi za adhabu hizi zitatokea katika sura 7:134.

Aya 132. Watu wa Firauni wakajisingizia kufahamu ya kuwa misiba iliyowafikia ni kwa sababu ya nuhusi mbaya iliyokuja na Musa. Hivi ndivyo wasemavyo wasioamini. Mjumbe wa Mungu anapofika, misiba inawafikia kwa sababu ya uovu wao. Badala ya kutubia dhambi zao, wanasema ati ni kisirani cha kufika Mjumbe wa Allah.

فَاَرْسَلْنَا عَلَيْهِمُ الطُّوْفَانَ وَالْجَرَادَ وَالْقُمَّلَ وَالضَّفَادِعَ وَالدَّمَ اٰيٰتٍ مُّفَصَّلٰتٍ فَاسْتَكْبَرُوْا وَكَانُوْا قَوْمًا مُّجْرِمِيْنَ ﴿١٣٣﴾

134. Ndipo Tukawapelekea tufani na nzige na chawa na vyura na damu kuwa Ishara zielezazo; lakini wakatakabari na walikuwa watu wakosefu.

وَلَمَّا وَقَعَ عَلَيْهِمُ الرِّجْزُ قَالُوْا يٰمُوْسَى ادْعُ لَنَا رَبَّكَ بِمَا عَهِدَ عِنْدَكَ ۚ لَئِنْ كَشَفْتَ عَنَّا الرِّجْزَ لَنُؤْمِنَنَّ لَكَ وَلَنُرْسِلَنَّ مَعَكَ بَنِيْٓ اِسْرَآءِيْلَ ﴿١٣٤﴾

135. Na ilipowaangukia adhabu, wakasema: Ewe Musa, tuombee kwa Mola wako yale Aliyokuahidi; kama ukituondolea adhabu, bila shaka tutakuamini na kwa yakini tutawapeleka wana wa Israeli pamoja nawe.

فَلَمَّا كَشَفْنَا عَنْهُمُ الرِّجْزَ اِلٰٓى اَجَلٍ هُمْ بٰلِغُوْهُ اِذَا هُمْ يَنْكُثُوْنَ ﴿١٣٥﴾

136. Lakini Tulipowaondolea adhabu kwa muda watakaoufikia, mara wakavunja ahadi.

فَانْتَقَمْنَا مِنْهُمْ فَاَغْرَقْنٰهُمْ فِي الْيَمِّ بِاَنَّهُمْ كَذَّبُوْا بِاٰيٰتِنَا وَكَانُوْا عَنْهَا غٰفِلِيْنَ ﴿١٣٦﴾

137. Basi Tukalipiza kisasi kwao na Tukawazamisha baharini kwa sababu walizikadhibisha Ishara Zetu na walikuwa si wenye kuziangalia.

وَاَوْرَثْنَا الْقَوْمَ الَّذِيْنَ كَانُوْا يُسْتَضْعَفُوْنَ مَشَارِقَ الْاَرْضِ وَمَغَارِبَهَا الَّتِيْ بٰرَكْنَا فِيْهَا ۭ وَتَمَّتْ كَلِمَتُ رَبِّكَ الْحُسْنٰى عَلٰي بَنِيْٓ اِسْرَآءِيْلَ ۙ بِمَا صَبَرُوْا ۭ وَدَمَّرْنَا مَا كَانَ يَصْنَعُ فِرْعَوْنُ وَقَوْمُهٗ وَمَا كَانُوْا يَعْرِشُوْنَ ﴿١٣٧﴾

138. Na Tukawarithisha watu waliokuwa wanaonekana dhaifu mashariki ya ardhi na magharibi yake ambayo Tuliibariki. Na likatimia neno jema la Mola wako kwa wana wa Israeli, kwa sababu walivumilia; na Tukayaangamiza yale aliyokuwa ameyatengeneza Firauni na watu wake, na pia yale waliyokuwa wakiyajenga.

وَجٰوَزْنَا بِبَنِيْٓ اِسْرَآءِيْلَ الْبَحْرَ فَاَتَوْا عَلٰي قَوْمٍ يَّعْكُفُوْنَ عَلٰٓى اَصْنَامٍ لَّهُمْ ۚ

139. Na Tukawavusha wana wa Israeli bahari, na wakawafikia watu waliokuwa wakiyaabudu masanamu yao.

Aya 134. Aya hii inaeleza namna mbili za adhabu zilizosemwa katika sura 7:131.Nzige na tufani huleta njaa; na chawa na vyura na damu huleta magonjwa yanayoleta vifo.

Aya 136. *Ajal,* "Muda," pia maana yake ni "mwisho wa muda." Tazama sura 2:232. Adhabu ¡liondolewa kwa muda tu ili kumpa Firauni nafasi ya kutubu na kukubali anayoyataka Musa.

Aya 138. *Mashariki ya ardhi na magharibi yake.* Kwa usemi wa Kiarabu, maneno hayo maana yake ni nchi nzima.

Aya 139. Ingawa neno *al-Bahar* na *al-Yamm* yanafahamiwa kuwa na maana moja, lakini ni

لَّهُمْ ۚ قَالُوْا يٰمُوْسَى اجْعَلْ لَّنَآ اِلٰهًا كَمَا لَهُمْ اٰلِهَةٌ ؕ قَالَ اِنَّكُمْ قَوْمٌ تَجْهَلُوْنَ ﴿۱۳۸﴾

Wakasema: Ewe Musa utufanyie mungu kama walivyo na miungu. Akasema: Hakika ninyi ni watu mfanyao ujinga.

اِنَّ هٰٓؤُلَآءِ مُتَبَّرٌ مَّا هُمْ فِيْهِ وَ بٰطِلٌ مَّا كَانُوْا يَعْمَلُوْنَ ﴿۱۳۹﴾

140. Hakika wanayoyashika hawa yataangamia, na ni bure waliyokuwa wakiyafanya.

قَالَ اَغَيْرَ اللّٰهِ اَبْغِيْكُمْ اِلٰهًا وَّ هُوَ فَضَّلَكُمْ عَلَى الْعٰلَمِيْنَ ﴿۱۴۰﴾

141. Akasema: Je, niwatafutieni mungu badala ya Allah hali Yeye Amewafadhilini kuliko walimwengu.

وَ اِذْ اَنْجَيْنٰكُمْ مِّنْ اٰلِ فِرْعَوْنَ يَسُوْمُوْنَكُمْ سُوْٓءَ الْعَذَابِ ۚ يُقَتِّلُوْنَ اَبْنَآءَكُمْ وَ يَسْتَحْيُوْنَ نِسَآءَكُمْ ؕ وَ فِيْ ذٰلِكُمْ بَلَآءٌ مِّنْ رَّبِّكُمْ عَظِيْمٌ ﴿۱۴۱﴾ ع

142. Na (kumbukeni) Tulipowaokoeni kwa watu wa Firauni waliowapeni adhabu mbaya, wakiwaua wavulana wenu na kuwaacha hai wanawake wenu; na katika hayo lilikuwa jaribio kubwa lililotoka kwa Mola wenu

FUNGU 17

وَ وٰعَدْنَا مُوْسٰى ثَلٰثِيْنَ لَيْلَةً وَّ اَتْمَمْنٰهَا بِعَشْرٍ فَتَمَّ مِيْقَاتُ رَبِّهٖٓ اَرْبَعِيْنَ لَيْلَةً ۚ وَ قَالَ مُوْسٰى لِاَخِيْهِ هٰرُوْنَ اخْلُفْنِيْ فِيْ قَوْمِيْ وَ اَصْلِحْ وَ لَا تَتَّبِعْ سَبِيْلَ الْمُفْسِدِيْنَ ﴿۱۴۲﴾

143. Na Tulimuahidi Musa siku thelathini na Tukazitimiza kwa kumi; ndipo ikatimia miadi ya Mola wake ya siku arobaini. Na Musa akamwambia ndugu yake Harun: Shika mahali pangu katika watu wangu na urekebishe wala usifuate njia ya waharibifu.

وَ لَمَّا جَآءَ مُوْسٰى لِمِيْقَاتِنَا وَ كَلَّمَهٗ رَبُّهٗ ۙ قَالَ رَبِّ اَرِنِيْٓ اَنْظُرْ اِلَيْكَ ؕ قَالَ لَنْ

144. Na alipofika Musa kwenye miadi Yetu, na Mola wake Akazungumza naye, (Musa) akasema: Mola wangu, nionyeshe ili nikuone.

---

dhahiri ya kuwa Qur'an inatumia neno *al-Yamm* inapoelezea kuzamishwa kwa watu wa Firauni (sura 7:137), na inatumia neno *al-Bahr* (kama katika Aya hii) inapoelezea habari ya Waisraeli kuivuka bahari. Hii ni kwa sababu neno *al-Bahr* kwa desturi huonyesha upana, na neno *al-Yamm* huonyesha kilindi.

Aya 140. Neno "hawa" ni wale waabudu masanamu ambao Waisraeli walitaka kuwaiga. Nabii Musa anawaeleza watu wake ya kwamba watu wanaotaka kuwaiga ni watu watakaoangamia.

Aya 143. *Shika mahali pangu katika watu wangu.* Maneno haya yanaonyesha kuwa Nabii Harun alikuwa chini ya amri ya Nabii Musa.

تَرٰىنِيْ وَلٰكِنِ انْظُرْ اِلَى الْجَبَلِ فَاِنِ
اسْتَقَرَّ مَكَانَهٗ فَسَوْفَ تَرٰىنِيْ ۚ فَلَمَّا
تَجَلّٰى رَبُّهٗ لِلْجَبَلِ جَعَلَهٗ دَكًّا وَّخَرَّ
مُوْسٰى صَعِقًا ۚ فَلَمَّآ اَفَاقَ قَالَ
سُبْحٰنَكَ تُبْتُ اِلَيْكَ وَاَنَا اَوَّلُ
الْمُؤْمِنِيْنَ ﴿١٤٣﴾

Akasema: Huwezi kuniona, lakini tazama jabali, kama litakaa mahali pake ndipo utaweza kuniona. Basi Mola wake Alipojidhihirisha kwenye jabali Akalifanya kuvunjikavunjika, na Musa akaanguka hali ya kuzimia; na alipozinduka akasema: Wewe Ndiwe Mtukufu, natubu Kwako, na mimi ni wa kwanza wa waaminio.

قَالَ يٰمُوْسٰٓى اِنِّى اصْطَفَيْتُكَ عَلَى
النَّاسِ بِرِسٰلٰتِىْ وَبِكَلَامِىْ ۖ فَخُذْ
مَآ اٰتَيْتُكَ وَكُنْ مِّنَ الشّٰكِرِيْنَ ﴿١٤٤﴾

145. Akasema: Ewe Musa hakika Nimekuchagua juu ya watu kwa risala Zangu na maneno Yangu; basi yashike Ninayokupa, na uwe miongoni mwa wanaoshukuru.

وَكَتَبْنَا لَهٗ فِى الْاَلْوَاحِ مِنْ كُلِّ شَىْءٍ
مَّوْعِظَةً وَّتَفْصِيْلًا لِّكُلِّ شَىْءٍ ۚ فَخُذْهَا
بِقُوَّةٍ وَّاْمُرْ قَوْمَكَ يَاْخُذُوْا بِاَحْسَنِهَا ۭ
سَاُورِيْكُمْ دَارَ الْفٰسِقِيْنَ ﴿١٤٥﴾

146. Na Tukamwandikia katika mbao mawaidha ya kila namna, na maelezo ya kila jambo. Basi yashike imara na uwaamuru watu wako washike yaliyo bora katika hayo. Hivi karibuni Nitawaonyesheni makao ya wavunjao amri.

سَاَصْرِفُ عَنْ اٰيٰتِىَ الَّذِيْنَ يَتَكَبَّرُوْنَ فِى
الْاَرْضِ بِغَيْرِ الْحَقِّ ۭ وَاِنْ يَّرَوْا كُلَّ اٰيَةٍ
لَّا يُؤْمِنُوْا بِهَا ۚ وَاِنْ يَّرَوْا سَبِيْلَ الرُّشْدِ
لَا يَتَّخِذُوْهُ سَبِيْلًا ۚ وَاِنْ يَّرَوْا سَبِيْلَ
الْغَيِّ يَتَّخِذُوْهُ سَبِيْلًا ۭ ذٰلِكَ بِاَنَّهُمْ
كَذَّبُوْا بِاٰيٰتِنَا وَكَانُوْا عَنْهَا غٰفِلِيْنَ ﴿١٤٦﴾

147. Nitawaepusha katika Ishara Zangu wale wanaotakabari katika nchi pasipo haki; na hata wakiona kila Ishara hawataiamini; na kama wakiiona njia ya mwongozo, hawaishiki kuwa njia; lakini wakiiona njia ya upotevu, wanaishika kuwa njia. Hayo ni kwa sababu walizikadhibisha Aya Zetu na walikuwa hawazijali.

Aya 146. *Tukamwandikia.* Si mradi wake kuwa Mungu aliandika amri zile kwa mkono Wake. Maneno kama haya yametumika mahali pengine kwa ajili ya Zaburi (sura 21:106). Kwa hakika ni Musa mwenyewe aliyeandika amri zile alizofunuliwa, juu ya ubao; lakini kwa kuwa Mungu ndiye aliyeziteremsha, basi imesemwa Yeye ameziandika. Kadhalika neno hili *katabnaa* (Tukamwandikia) linaweza kuwa na maana ya "Tukaamrisha."

Maelezo ya kila jambo, na *kila namna*. Mradi wake ni, kila jambo lililotakiwa kwa ajili ya kuwaongoza Waisraeli wakati ule.

148. Na wale waliozikadhibisha Ishara Zetu na mkutano wa Akhera, vitendo vyao vimeharibika. Hawatalipwa ila yale yale waliyokuwa wakiyatenda.

وَالَّذِيْنَ كَذَّبُوْا بِاٰيٰتِنَا وَلِقَآءِ الْاٰخِرَةِ حَبِطَتْ اَعْمَالُهُمْ ؕ هَلْ يُجْزَوْنَ اِلَّا مَا كَانُوْا يَعْمَلُوْنَ ﴿۱۴۷﴾ ع

FUNGU 18

149. Na baada yake watu wa Musa wakafanya katika mapambo yao kiwiliwili cha ndama kilichokuwa na sauti. Je, hawakuona ya kwamba yeye hasemi nao wala hawaongozi njia? Walimtwaa kuwa mungu na wakawa wenye kudhulumu.

وَاتَّخَذَ قَوْمُ مُوْسٰى مِنْۢ بَعْدِهٖ مِنْ حُلِيِّهِمْ عِجْلًا جَسَدًا لَّهٗ خُوَارٌ ؕ اَلَمْ يَرَوْا اَنَّهٗ لَا يُكَلِّمُهُمْ وَلَا يَهْدِيْهِمْ سَبِيْلًا ۘ اِتَّخَذُوْهُ وَكَانُوْا ظٰلِمِيْنَ ﴿۱۴۸﴾

150. Na walipojuta na wakaona ya kwamba wamekwisha potea, wakasema: Kama asingeturehemu Mola wetu na kutusamehe, bila shaka tungalikuwa miongoni mwa wapatao hasara.

وَلَمَّا سُقِطَ فِيْۤ اَيْدِيْهِمْ وَرَاَوْا اَنَّهُمْ قَدْ ضَلُّوْا ۙ قَالُوْا لَئِنْ لَّمْ يَرْحَمْنَا رَبُّنَا وَيَغْفِرْ لَنَا لَنَكُوْنَنَّ مِنَ الْخٰسِرِيْنَ ﴿۱۴۹﴾

151. Na aliporudi Musa kwa watu wake, akiwa amekasirika na kusikitika, akasema: Ni maovu mliyonifanyia nyuma yangu. Je, mmeitangulia amri ya Mola wenu? Na akaweka mbao na akakamata kichwa cha nduguye akikivutia kwake. Yeye akasema: Ewe mwana wa mama yangu, kwa hakika watu (hawa) wameniona dhaifu na hata walikuwa karibu kuniua, basi usiwafurahishe maadui juu yangu, wala usiniweke pamoja na watu wadhalimu.

وَلَمَّا رَجَعَ مُوْسٰۤى اِلٰى قَوْمِهٖ غَضْبَانَ اَسِفًا ۙ قَالَ بِئْسَمَا خَلَفْتُمُوْنِيْ مِنْۢ بَعْدِيْ ۚ اَعَجِلْتُمْ اَمْرَ رَبِّكُمْ ۚ وَاَلْقَى الْاَلْوَاحَ وَاَخَذَ بِرَاْسِ اَخِيْهِ يَجُرُّهٗۤ اِلَيْهِ ؕ قَالَ ابْنَ اُمَّ اِنَّ الْقَوْمَ اسْتَضْعَفُوْنِيْ وَكَادُوْا يَقْتُلُوْنَنِيْ ۖ فَلَا تُشْمِتْ بِيَ الْاَعْدَآءَ وَلَا تَجْعَلْنِيْ مَعَ الْقَوْمِ الظّٰلِمِيْنَ ﴿۱۵۰﴾

Aya 149. Ndama anakanushwa kuwa si Mungu kwa sababu hawezi kuzungumza na wafuasi wake wala hawezi kuwaongoza namna yo yote. Hii inaonyesha ya kwamba Mungu anaweza kuwa Mungu wa kweli maadam anasema na watumishi Wake na kuwatolea njia za kuwaongoza. Tazama sura 20:90.

Aya 151. Musa alishika kichwa cha Harun si kwa sababu, kama isemavyo Biblia, ya kwamba Harun alikuwa nao shauri moja katika kumwabudu ndama yule (Kutoka 32:2-4), bali ni kwa sababau alishindwa kuwazuia wasimwabudu ndama.

Musa kumtendea Harun vile haiwezi kusemwa ni tabia mbaya. Hasira ya Musa ilikuwa na haki kwa sababu kufuru kubwa ilifanyika, na kazi ile ya maisha yake yote ikaharibiwa. Hivyo alikuwa na haki kabisa kukasirika.

قَالَ رَبِّ اغْفِرْ لِيْ وَلِاَخِيْ وَاَدْخِلْنَا فِيْ رَحْمَتِكَ ۖ وَاَنْتَ اَرْحَمُ الرّٰحِمِيْنَ ﴿١٥١﴾

152. Akasema (Musa): Mola wangu, nisamehe mimi na ndugu yangu, na Utuingize katika rehema Zako, maana Wewe ndiwe Mrehemevu zaidi kuliko wanaorehemu.

FUNGU 19

اِنَّ الَّذِيْنَ اتَّخَذُوا الْعِجْلَ سَيَنَالُهُمْ غَضَبٌ مِّنْ رَّبِّهِمْ وَذِلَّةٌ فِي الْحَيٰوةِ الدُّنْيَا ۭ وَكَذٰلِكَ نَجْزِي الْمُفْتَرِيْنَ ﴿١٥٢﴾

153. Hakika wale waliomtwaa ndama (kuwa mungu), hivi karibuni itawafikia hasira kutoka kwa Mola wao na fedheha katika maisha ya dunia; na hivi ndivyo Tunavyowalipa watungao uwongo.

وَالَّذِيْنَ عَمِلُوا السَّيِّاٰتِ ثُمَّ تَابُوْا مِنْۢ بَعْدِهَا وَاٰمَنُوْٓا ۙ اِنَّ رَبَّكَ مِنْۢ بَعْدِهَا لَغَفُوْرٌ رَّحِيْمٌ ﴿١٥٣﴾

154. Na wale waliofanya matendo mabaya, kisha wakatubu baada yake na kuamini, kwa yakini Mola wako, baada ya haya, ni Msamehevu, Mrehemevu.

وَلَمَّا سَكَتَ عَنْ مُّوْسَى الْغَضَبُ اَخَذَ الْاَلْوَاحَ ۖ وَفِيْ نُسْخَتِهَا هُدًى وَّرَحْمَةٌ لِّلَّذِيْنَ هُمْ لِرَبِّهِمْ يَرْهَبُوْنَ ﴿١٥٤﴾

155. Na ilipotulia ghadhabu ya Musa akazitwaa zile mbao na katika maandiko yao ulikuwamo mwongozo na rehema kwa wale wanaomwogopa Mola wao.

وَاخْتَارَ مُوْسٰى قَوْمَهٗ سَبْعِيْنَ رَجُلًا لِّمِيْقَاتِنَا ۚ فَلَمَّآ اَخَذَتْهُمُ الرَّجْفَةُ قَالَ رَبِّ لَوْ شِئْتَ اَهْلَكْتَهُمْ مِّنْ قَبْلُ وَاِيَّايَ ۭ اَتُهْلِكُنَا بِمَا فَعَلَ السُّفَهَاۗءُ مِنَّا ۚ اِنْ هِيَ اِلَّا فِتْنَتُكَ ۭ تُضِلُّ بِهَا مَنْ تَشَاۗءُ وَتَهْدِيْ مَنْ تَشَاۗءُ ۭ اَنْتَ وَلِيُّنَا فَاغْفِرْ لَنَا وَارْحَمْنَا وَاَنْتَ خَيْرُ الْغٰفِرِيْنَ ﴿١٥٥﴾

156. Na Musa akawachagua watu sabini katika kaumu yake kwa miadi Yetu; na lilipowashika tetemeko la ardhi akasema: Mola wangu, kama Ungetaka Ungaliwaangamiza wao na mimi zamani. Je, Utatuangamiza kwa sababu ya yale waliyofanya wapumbavu kati yetu? Siyo haya ila ni majaribio Yako, kwayo Humpoteza Umtakaye na Kumuongoza Umtakaye. Wewe ndiwe Mlinzi wetu, basi tusamehe na Uturehemu, nawe ndiwe Mbora wa kughofiri.

Neno *ma'a* (pamoja na) ambalo limetumiwa katika Aya: *Wala usiniweke pamoja na watu wadhalimu,* linasaidia kufafanua maana ya neno hilo katika sura 4:70. Hapa neno hili maana yake ni "miongoni mwa."

وَاكْتُبْ لَنَا فِيْ هٰذِهِ الدُّنْيَا حَسَنَةً وَّفِي
الْاٰخِرَةِ اِنَّا هُدْنَآ اِلَيْكَ ؕ قَالَ عَذَابِيْٓ
اُصِيْبُ بِهٖ مَنْ اَشَآءُ ۚ وَرَحْمَتِيْ
وَسِعَتْ كُلَّ شَيْءٍ ؕ فَسَاَكْتُبُهَا لِلَّذِيْنَ
يَتَّقُوْنَ وَيُؤْتُوْنَ الزَّكٰوةَ وَالَّذِيْنَ هُمْ
بِاٰيٰتِنَا يُؤْمِنُوْنَ ﴿۱۵۶﴾

157. Na Utuandikie mema katika dunia hii na katika Akhera; bila shaka tumeelekea Kwako. Akasema: Adhabu Yangu Nitamfikishia Nimtakaye, na rehema Yangu hukienea kila kitu; basi Nitaiandika kwa ajili ya wale wanaoogopa na kutoa Zaka na wale wanaoziamini Aya Zetu,

اَلَّذِيْنَ يَتَّبِعُوْنَ الرَّسُوْلَ النَّبِيَّ الْاُمِّيَّ
الَّذِيْ يَجِدُوْنَهٗ مَكْتُوْبًا عِنْدَهُمْ
فِي التَّوْرٰىةِ وَالْاِنْجِيْلِ ۫ يَاْمُرُهُمْ
بِالْمَعْرُوْفِ وَيَنْهٰىهُمْ عَنِ الْمُنْكَرِ
وَيُحِلُّ لَهُمُ الطَّيِّبٰتِ وَيُحَرِّمُ عَلَيْهِمُ
الْخَبٰٓئِثَ وَيَضَعُ عَنْهُمْ اِصْرَهُمْ
وَالْاَغْلٰلَ الَّتِيْ كَانَتْ عَلَيْهِمْ ؕ فَالَّذِيْنَ
اٰمَنُوْا بِهٖ وَعَزَّرُوْهُ وَنَصَرُوْهُ وَاتَّبَعُوا
النُّوْرَ الَّذِيْٓ اُنْزِلَ مَعَهٗٓ ۙ اُولٰٓئِكَ هُمُ
الْمُفْلِحُوْنَ ﴿۱۵۷﴾ ع

158. Ambao wanamfuata Mtume, Nabii aliye Ummi, ambaye wao humkuta ameandikwa kwao katika Taurati na Injili, Huwaamuru yaliyo mema na huwakataza yaliyo mabaya, na huwahalalishia vitu vizuri na huwaharimishia vitu vibaya, na huwaondolea mizigo yao na minyororo iliyokuwa juu yao. Ama wale waliomuamini yeye na kumheshimu na kumsaidia na wakaifuata nuru iliyoteremshwa pamoja naye, hao ndio wenye kufaulu.

Aya 158. *Ambao wanamfuata Mtume, Nabii aliye Ummi,* yaani Mtume Muhammad *s.a.w.* Neno *ummi* maana yake ni "anayehusiana na mama," yaani asiye na kosa kama alivyo mtoto anayenyonya kifuani pa mama yake. Neno hilo pia maana yake ni mtu, hasa Mwarabu, asiye na Kitabu kilichoteremshwa na Mwenyezi Mungu; mtu asiyejua kusoma na kuandika; mtu wa mji wa Makka ambao unaitwa *Ummul-Quraa* (Mama wa miji).

Ameandikwa kwao katika Taurati na Injili. Kila Nabii huwaambia wafuasi wake kumwamini Mtume wa Mungu atakayekuja baada yake. Mtume Muhammad *s.a.w.* kwa kuwa ni mbora wa Mitume wote (sura 33:41, maelezo), tena kwa kuwa alitumwa kwa mataifa yote (sura 7:159), bishara zinazotabiri kuja kwake zinapatikana katika vyuo vya dini zote. Hapa vimetajwa Taurati na Injili. Katika Vyuo hivyo mna bishara nyingi zenye kuwawezesha Mayahudi na Wakristo kumtambua Mtume *s.a.w.* Hapa tutaeleza bishara chache:

BISHARA YA KWANZA.

Siku ya mkutano katika Horeb, wana wa Israeli walipokataa kusikia sauti ya Allah, Mungu akamwambia Musa, "Wametenda vyema kusema walivyosema. Mimi nitawaondokeshea Nabii miongoni mwa ndugu zao mfano wako wewe, nami nitatia maneno yangu kinywani mwake, naye atawaambia yote nitakayomwamuru. Hata itakuwa, mtu asiyesikiliza maneno yangu atakayosema yule kwa jina langu, nitalitaka kwake. Lakini Nabii atakayenena neno kwa kujikinai kwa jina langu, ambalo sikumwagiza kulinena, au atakayenena katika jina la miungu mingine, nabii yule atakufa" (Kumbukumbu 18:16-20).Bishara hii tukufu inaonyesha mambo haya yafua--tayo;

(i) Wana wa Israeli hawatasikia tena sauti yenye nguvu ya Allah.
(ii) Anayebashiriwa kufika ni Nabii
(iii) Ataondokeshwa miongoni mwa ndugu wa Waisraeli
(iv) Atakuwa mfano wa Musa.
(v) Maneno atakayosema yatakuwa ufunuo wa Mungu.
(vi) Atawaambia yote atakayoambiwa na Mungu.
(vii) Atanena hayo kwa jina la Mungu.
(viii) Asiyetaka kusikiliza maneno yake ataadhibiwa.
(ix) Nabii wa uwongo, atakayesingizia kutumwa na Mungu, atakufa
(x) Atakayesema kwa jina la miungu wengine pia atauawa.

Sasa, ni watu wawili wanaosemwa kuwa wameaguliwa na bishara hiyo. Wakristo wanasema ni Yesu, na Waislamu tunasema ni Muhammad s.a.w. Bishara yenyewe haisemi jina la mtu ye yote, ila tu imeeleza alama kumi za Nabii huyo. Basi tupeleleze alama hizo zinamwangukia nani katika hawa Manabii wawili.

(i) Katika bishara hiyo Waisraeli wanaambiwa ya kwamba hawatasikia tena sauti ya Mungu. Na inajulikana pote ya kuwa Yesu alikuwa Mwisraeli, aliyezaliwa katika ukoo wa Daudi (Matt. 1:1). Mtume *s.a.w.* alikuwa Mwarabu. Hakuwa katika kizazi cha Waisraeli kilichonyimwa baraka za Mungu kwa kukataa kwao kusikia sauti ya Mungu.

(ii) Bishara inasema ya kuwa huyo aliyebashiriwa kufika atakuwa Nabii. Wakristo wanaamini kuwa Yesu alikuwa "Mungu Mwana" Mtume *s.a.w*. alijiita *Rasuulullaahi* (Mtume wa Mungu) na pia *Nabiyyullaahi* (Nabii wa Mungu).

(iii) Ikumbukwe ya kuwa Mtume *s.a.w.* alizaliwa katika ukoo wa Ismaili, nduguye Isihaka. Wazao wa Ismaili ndio Waarabu; na watoto wa Yakubu, mwanawe Isihaka wanaitwa Waisraeli. Mtume *s.a.w* ametokana na Waismaili ambao ni ndugu za Waisraeli, kama inavyoagua bishara. Lakini Yesu mwenyewe ni Mwisraeli, hakutoka katika ndugu za Waisraeli. Hivyo bishara hii si yake.

(iv) Bishara inaeleza tena ya kuwa Mtume huyo atakuwa mfano wa Musa. Nasi tunaona ya kuwa Mtume Muhammad *s.a.w.* ndiye ameitwa mfano wa Musa katika Qur'an (sura 73:16). Yesu angewezaje kujifanya kama Musa hali mwenyewe alikuwa chini ya sheria ya Musa? (Soma Matt. 5:17; 7:12; Marko 10:19; Matendo 24:14). Hali ya Mtume Muhammad *s.a.w.* na ya Nabii Musa zinafanana sana. Nabii Musa alizaliwa na wazazi wawili, wala hakulaumiwa katika kuzaliwa kwake; tena Musa alioa; alipewa Sheria mpya; alihama nchi yake baada ya kupewa Utume; alipigana na adui zake; nao wakaangamia mbele ya macho yake; alikufa kifo cha kawaida; walitokea maimamu na mawalii katika umati wake: na mwishowe, alikuja Masihi kuisimamisha Sheria ya Musa. Hayo yalipatikana kwa Mtume Muhammad *s.a.w.* na hivyo wamefanana kabisa. Lakini hakuna katika alama hizo hata moja inayopatikana katika maisha ya Yesu.

(v) Bishara inaendelea kusema, "Nami nitatia maneno yangu kinywani mwake." Yaani, Mungu atamteremshia maneno yake. Alama hii pia haionekani katika Yesu. Wakristo wanaamini ya kwamba Yesu alikuwa Mungu, kwa hiyo hakuwa na haja ya kufunuliwa maneno kutoka kwa Mungu. Zaidi ya hayo Qur'an ndio Sheria ya pekee inayostahiki kuitwa "Maneno ya Mungu," maana haina hata neno moja lisilotoka kwa Mungu Mwenye enzi.

(vi) Mtume *s.a.w* anaambiwa na Allah kufikisha yote aliyoteremshiwa (sura 5:68). Yesu aliwaambia wanafunzi wake ya kwamba hatawaeleza yote (Yohana 19:12, 13). Na bishara inasema, yule Nabii atawaambia yote atakayoamriwa na Mungu. Hivyo bishara hii haimhusu Yesu.

(vii) Alama ya saba pia haionekani katika Yesu. Mtu anayesoma Injili anajua ya kwamba Injili yo yote haikuanzishwa kwa jina la Mungu. Yesu anasema mara kwa mara, "Bali mimi nawaambieni" (Matt. 5:22, 28, 34, 39, 44). Luka anasema ameandika Injili yake kwa sababu, "Nimeona vema mimi nami, kwa kuwa nimejitafutia usahihi wa mambo hayo yote tangu mwanzo, kukuandikia kwa taratibu, Theofilo Mtukufu" (Luka 1:3, 4). Hasemi kwamba alifunuliwa na

Mungu, au ameongozwa na Roho Mtakatifu; wala hakuandika Injili hiyo ili watu wote waisome; bali alimwandikia mtu mmoja tu, Theofilo. Paulo alisema, "Kwa habari za wanawali, sina amri ya Bwana, lakini natoa shauri langu" (1 Wakor. 7:25). Ni dhahiri ya kwamba Injili za leo ni mchanganyiko wa maneno ya watu mbalimbali. Lakini Qur'an inataja jina la Mungu mwanzo wa kila sura, na inaonekana Allah alikusudia kutimiza alama hiyo waziwazi. Tena Mtume *s.a.w.* kabla ya kuanza kazi yo yote alikuwa anataja jina la Allah.

(viii) Waliokataa kusikiliza maneno ya Mungu yaliyotoka kinywani mwa Mtume *s.a.w.* waliadhibiwa hapahapa duniani.Vita vikali vilivyoangamiza maadui wa Uislam vilikuwa adhabu ya Allah iliyoahidiwa katika bishara hii, na bado kuna adhabu ya Akhera itakayowawakia watu wanaoiadui haki.

(ix) Wapinzani wa Uislamu wanasema ya kwamba Mtume *s.a.w* alizua uwongo. Bishara hii inawajibu na kusema, mtu ye yote amzuliaye Mungu atauawa. Mtume *s.a.w* alikaa miaka mingi duniani, alipokwisha maliza kazi yake,akafa kifo cha kawaida.Lakini Yesu je?Tukifuata imani ya Wakristo ya kusema kuwa aliuawa msalabani tutashurutishwa kusema ya kuwa (Mungu apishe mbali) alikuwa mwongo; maana bishara inasema ya kuwa nabii wa uwongo ndiye atauawa. Hivyo, kufaulu kwa Mtume *s.a.w.* na maendeleo ya kazi yake ni dalili zilizo wazi za ukweli wake.

(x) Bishara inaeleza tena ya kuwa mwenye kusema neno kwa jina la miungu wengine, "nabii yule atakufa." Kwa kuwa Mtume hakuuawa, basi imethibitika ya kwamba yote aliyosema alifunuliwa na Mungu.

BISHARA YA PILI.

Katika Kumbukumbu la Taurati 33:2, 3 imeandikwa hivi: "BWANA alitoka Sinai, Akawaondokea kutoka Seiri; Akaangaza kutoka kilima cha Parani, na akaja na elfu kumi za watakatifu. Upande wa mkono wake wa kuume palikuwa na sheria motomoto kwao. Hakika awapenda hayo makabila ya watu: watakatifu wake wote wamo mkononi mwako; nao waliketi miguuni pako."

Hapa pameelezwa maonyesho matatu ya Allah. Musa alitoka Sinai. Seiri ni alama ya Yesu. Na Mtume Muhammad *s.a.w.* aliangaza kutoka kilima cha Parani. Wanazuoni wamekubali ya kwamba Parani ni kilima cha Makka (Mu'jamul Buldaan). Biblia inasema, Ismaili "akakaa katika jangwa la Parani" (Mwanzo 21:21); na Mtume Muhammad *s.a.w.* ni mjukuu wa Ismaili.

Mtume *s.a.w.* alipotoka Madina kwenda ishika Makka, alikuwa na masahaba elfu kumi. Katika Biblia ya Kiingereza hesabu ya watakatifu hao imetajwa kuwa "ten thousands of saints," yaani, "elfu kumi za watakatifu" kama tulivyofasiri hapo juu. Lakini katika Biblia ya Kiswahili cha Mvita (Mombasa), wamefasiri maneno hayo kuwa "makumi ya maelfu," yaani elfu zile zilikuwa si kumi moja, bali makumi mengi; ili wapate kuwavuruga wasomao Kiswahili wasijue hesabu ya masahaba watakatifu wa Mtume *s.a.w.* aliotokea nao Parani iliyotajwa barabbara katika bishara ya Biblia.

Inasikitisha kuona ya kwamba mapadre hawajatosheka na kiasi hicho cha mageuzi. Katika tafsiri mpya ya Biblia (Union Version) ya mwaka 1952, kifungu hicho cha maneno wamekiandika hivi: "Akaja Meribath-kadeshi" ili wavuruge kabisa bishara hiyo isifafanuke. Ni ajabu ya kuwa maneno kama *Tirshatha* (uk. 478), *Darkoni* (uk. 479) na mengineyo yameelezwa chini katika kurasa, na mengine yameelezwa mwisho wa kitabu cha Biblia. Lakini neno *Meribath-kadeshi* hawakulieleza chini ya ukurasa ule, wala mwisho wa kitabu. Ingawa ni jipya kabisa lakini limefanywa lionekane kama jina la mtu au Malaika au hivi. Wale wanaofikiri Biblia ya Union Version imefasirika vizuri sana katika Kiswahili cha kisasa, watasemaje juu ya uaminifu huu wa wafasiri? Ilikuwaje wanazuoni wakubwa-wakubwa wa Kiyunani na Kihebrania na Kiswahili kushindwa kutafsiri au kueleza neno *Meribath-kadeshi?* Inaonekana dhahiri ya kwamba dhamiri za mapadre zinawalaumu juu ya tafsiri zao zisizo sahihi, zinazovurugwa makusudi ili kuficha haki.

Alama nyingine ni kuleta Sheria. Mtume Muhammad *s.a.w.* ndiye aliyeleta Sheria baada ya Nabii Musa.Na ile Sheria ilileta joto katika mioyo ya Waislamu,nao wakainuka katika miaka michache. Pia imeitwa "Sheria ya moto-moto" kwa ajili ya kuunguza uovu, madhambi na mabaya yote. Wale waliojaribu kuipinga Qur'an wakaangamia wenyewe. Kweli, Qur'an ikifuatwa sawasawa, inaweza kuchoma dhambi za watu kama moto unavyochoma takataka. Je hamwoni Waarabu waliokuwa wakinywa ulevi kutwa mara tano waliacha wakawa wanasali kutwa mara tano?

Mtume *s.a.w.* alizipenda sana kabila zote. Katika masahaba wake kulikuwa Waarabu wa makabila mbalimbali, watu wa Habeshi, Ajemi na Rumi, na Mtume *s.a.w.* aliwapenda wote. Hakuwaita mbwa na nguruwe watu wa mataifa kama alivyowaita Yesu (Matt. 7:6; 15:26).

Sahaba za Mtume pia walimpenda sana. Kwa hakika Mtume alipendwa na masahaba wake zaidi kuliko kila mtu anavyopendwa na wafuasi wake. Katika vita, kama mishale ilipigwa toka kila upande, masahaba walimzunguka Mtume kama kuta ili asipate kujeruhiwa. Hatuwezi kuwalinganisha na wanfunzi wa Yesu waliotoroka wote wakakimbia na kumwacha peke yake katika matata (Mathayo 26:56; Marko14:50).

BISHARA YA TATU.

Katika Wimbo ulio bora 5:10 mmeandikwa, "Mpenzi wangu ni mweupe tena mwekundumwekundu. Ndiye mkuu katika elfu kumi" (Biblia ya Kimvita). Huyu aliyetajwa hapa na Nabii Sulemani aliyekuwa mkuu katika watu elfu kumi si mwingine bali Mtume Muhammad *s.a.w.* Maneno ya mbele ya haya yameeleza sifa zote za mwili wa Mtume *s.a.w.* kama alivyokuwa.

BISHARA YA NNE.

Isaya 28:9-13 kinasema, "Atamfundisha nani maarifa? atamfahamisha nani habari hii? Je! ni wale walioachishwa maziwa, walioondolewa matitini? Kwa maana ni amri juu ya amri, amri juu ya amri; kanuni juu ya kanuni, kanuni juu ya kanuni; huku kidogo na huku kidogo. La, bali kwa midomo ya watu wageni, na kwa lugha nyingine atasema na watu hawa; ambao aliwaambia. Hii ndio raha yenu, mpeni raha yeye aliyechoka; huku ndiko kuburudika; lakini hawakutaka kusikia.

"Kwa sababu hiyo neno la BWANA kwao litakuwa hivi, amri juu ya amri; kanuni juu ya kanuni, kanuni juu ya kanuni; huku kidogo na huku kidogo; ili waende na kuanguka nyuma, na kuvunjwa, na kunaswa, na kuchukuliwa."

Walioachishwa maziwa na kuondolewa matitini ni wana wa Ismaili ambao waliakhirishwa kupata ujumbe wa Mungu. Qur'an iliteremshwa pole pole, amri juu ya amri, kama ielezavyo bishara hiyo. Baadhi ya sura zilishushwa Makka na nyingine Madina (Huku kidogo na huku kidogo). Qur'an iliteremka katika lugha ya Kiarabu ambayo ni "midomo ya watu wageni" kwa wana wa Israeli. Mbele imeelezwa ya kwamba Mtume atakimbilia Madina kwenye raha, mapumziko na maburudiko; lakini watu wa Makka watazidi kukataa ujumbe wa Uislamu, mpaka watashindwa, na kuvunjwa, na kunaswa na kuchukuliwa.

BISHARA YA TANO.

Injili ya Yohana inatuambia ya kwamba Mayahudi walitazamia Manabii watatu. Walituma watu kumwuliza Yohana mbatizaji, "Wewe u nani? Naye alikiri, wala hakukana; alikiri kwamba mimi siye Kristo. Wakamwuliza, ni nani basi? U Eliya wewe? Akasema: Mimi siye. Wewe u Nabii yule? Akajibu, La" (1:19-21).

Kristo, Eliya na Nabii Yule ndio Mitume watatu waliotazamiwa kufika, waliongojewa na Waisraeli. Injili inaeleza ya kwamba Yohana Mbatizaji ndiye Eliya (Matt. 17:10-13; Luka 1:18); na Kristo ni Yesu. Sasa amebaki mmoja, naye ni Nabii Yule, ambaye si mwingine ila ni Mtume Muhammad *s.a.w.;* maana hakuna baada ya Kristo mtu aliyedai kuwa bishara zake zimo katika Biblia, kisha akafaulu, isipokuwa Mtume Muhammad *s.a.w.* tu.

BISHARA YA SITA..

Yohana 14:16 imeandikwa, "Nami nitamwomba Baba naye atawapa Msaidizi mwingine, ili akae nanyi hata milele." Tena Yesu alisema, "Hayo ndio niliyowaambia wakati nilipokuwa nikikaa kwenu. Lakini huyo Msaidizi, Huyo Roho Mtakatifu, ambaye Baba atampeleka kwa jina langu, atawafundisha yote na kuwakumbusha yote niliyowaambia" (Yohana 14: 25-26). Tena Yesu alisema, "Hata bado nikali ninayo mengi ya kuwaambia, lakini hamwezi kuyastahamili hivi sasa. Lakini yeye atakapokuja huyo Roho wa Kweli, atawaongoza awaite kwenye kweli yote" (Yohana 16:12, 13).

Wakristo wanasema, "Msaidizi Mwingine" aliyeahidiwa kufika katika Injili ya Yohana si Mtume Muhammad, bali ni Roho Mtakatifu. Waislamu tunajibu Hivi:-

(i) Kama Msaidizi huyo ni Roho Mtakatifu, Yesu asingesema, "Yawafaa ninyi mimi niondoke; kwa maana mimi nisipoondoka, huyo Msaidizi hatakuja kwenu" (Yohana 16:7). Yesu asingesema hivyo kwa sababu huyo Roho Mtakatifu wa Wakristo alikuwako duniani siku zote, hata kabla ya Yesu kuzaliwa. Yesu alipobatizwa, Roho huyo alimshukia (Matt. 3:16). Tena kabla ya kuwaacha wanafunzi wake aliwapulizia, akawaambia: "Pokeeni Roho Mtakatifu" (Yohana 20:22). Ilmuradi, wanafunzi wa Yesu walikuwa na Roho huyo kabla ya kufa kwa Yesu, au tuseme, kabla hajatengana nao.

(ii) Zile alama zilizobainishwa na Yesu hazipatikani katika Roho Mtakatifu, kama (a) kuwaongoza watu kwenye kweli yote na kuwakumbusha maneno ya Yesu: na (b) kumtukuza Yesu (Yohana 16:14).

Mtume Muhammad *s.a.w.* ndiye aliyekuja miaka mingi baada ya Yesu, akileta Sheria yenye amri nyingi za Sheria za zamani, na mengi yaliyo mapya, ili kukamilisha Sheria. Qur'an yenyewe inadai kuwa Sheria iliyo kamili (sura 5:4). Tena Mtume *s.a.w.* alimtukuza Yesu na kumkinga na masingizio yote ya Mayahudi na Wakristo, akamwonyesha kama mtu mwema asiye na dhambi yo yote.

Ikiwa Wakristo wangali wanaongozwa na Roho Mtakatifu, mbona basi wanayo makanisa mbalimbali yanayopingana? Je, kila kanisa lina Roho Mtakatifu wake? Kisha kila Roho Mtakatifu wa kila kanisa anakuwa adui wa Roho Mtakatifu wa Kanisa jingine? Hata watu wa kanisa moja hawachelei kuwaita Wakristo wa kanisa jingine "Mpinga Kristo na watu wa Shetani.Au, je,Yesu akitoka mbinguni atakwenda na nani na ataacha nani katika wale ambao wamekwisha pata ubatizo au wanaopewa misa na sakramenti nyingine mara kwa mara, lakini ambao wanaitwa na Wakristo wakanisa jingine wapinga Kristo na watu wa Shetani? Hakika ni hii ya kuwa hawana dalili yo yote ya kuhakikisha kuwa yule Roho wa Kweli aliyeahidiwa ni Roho Mtakatifu wanayedhani kuwa wanaye anayewaongoza. Ni jambo wasiloweza kuhakikisha, iliyobaki ni madai ya mdomo tu.

BISHARA YA SABA.

Siku moja Petro aliwahotubia watu akasema, "Tubuni basi mrejee, ili dhambi zenu zifutwe, zipate kuja nyakati za kuburudishwa kwa kuwako kwake Bwana; apate kumtuma Kristo Yesu mliyewekewa tangu zamani; ambaye ilimpasa kupokewa mbinguni hata zije zamani za kufanywa upya vitu vyote, zilizonenwa na Mungu kwa kinywa cha Manabii wake watakatifu tokea mwanzo wa ulimwengu. Kwa maana Musa kweli alisema ya kwamba, Bwana Mungu wenu atawainulieni Nabii, katika ndugu zenu, kama mimi; msikieni yeye katika mambo yote atakayonena nanyi" (Matendo 3: 19-22).

Katika hotuba yake Petro ameeleza wakati wa kutimia ile bishara iliyotajwa katika Kumbukumbu la Taurati 18 iliyokwisha elezwa katika fungu (i) la maelezo haya. Anasema Yesu hana budi kukaa kwanza mbinguni hata maneno yaliyonenwa na Manabii yatimie. Inaoneka kama Petro hapatani na wale Wakristo wanaosema ya kwamba Yesu ndiye aliyetabiriwa na bishara hiyo. Anafikiri Nabii mwingine lazima aje baada ya kuondoka Yesu na kabla ya kurejea kwake mara ya pili. Mtume Muhammad *s.a.w.* ndiye aliyefika sawa na bishara hiyo.

FUNGU 20

159. Sema: Enyi watu, hakika mimi ni Mtume wa Allah kwenu nyote, Ambaye Anao ufalme wa mbingu na ardhi, hapana aabudiwaye ila Yeye,

قُلْ يَاَيُّهَا النَّاسُ اِنِّىْ رَسُوْلُ اللّٰهِ اِلَيْكُمْ جَمِيْعَا ۨ الَّذِىْ لَهٗ مُلْكُ السَّمٰوٰتِ

BISHARA YA NANE.

Katika barua aliyoandika Yuda (Yuda 1:14-15) tunasoma maneno haya: "Na Henoko, mtu wa saba baada ya Adamu, alitoa maneno ya unabii juu ya hao, akisema, Angalia, Bwana alikuja na watakatifu wake, maelfu maelfu, ili afanye hukumu juu ya watu wote, na kuwaadhibisha wote wasiomcha Mungu, kwa ajili ya kazi zao zote za upotevu walizozitenda bila kumcha Mungu, na kwa ajili ya maneno magumu yote ambayo hao wenye dhambi wasiomcha Mungu wameyanena juu yake."

Maneno ya juu tumeyanakili toka tafsiri mpya ya Biblia katika Kiswahili iitwayo "Union Version." Katika tafsiri hii mpya wameandika, "Bwana alikuja na watakatifu wake maelfu maelfu." Lakini katika tafsiri za zamani, katika Kiswahili mpaka mwaka 1949 walitafsiri "Elfu kumi za watakatifu wake." Kila mtu atafahamu ya kwamba hayo si tofauti ya maneno tu, bali maana pia imegeuzwa. Maana bishara hiyo inabashiria kufika kwa Mtume Muhammad pamoja na watakatifu elfu kumi, na ilitimia wakati Mtume alipoingia Makka na idadi hiyo ya watakatifu. Hakuna Nabii ye yote aliyetimiliwa na bishara hiyo isipokuwa Muhammad *s.a.w.* Ni kwa sababu hii mapadre wamependa kubadilisha maneno hayo ili kuwadanganya na kuwavuruga wasomao Kiswahili. Juu ya hayo, Injili za Kiingereza bado zina maneno "ten thousands of his saints" (elfu kumi za watakatifu wake).

NASAHA KWA WAKRISTO.

Wakristo wanaomwogopa Mungu watafahamu ya kuwa wamelazimika kumkubali Mtume Muhammad *s.a.w.*, hata kwa ushahidi wa hizi Injili zinazogeuzwa-geuzwa. Ingieni Uislamu kwa haraka ili msiadhibiwe na Allah kwa sababu ya kutojali bishara Zake. Mkikawia sana, pengine mtakuta bishara hizo zote zimekwisha kubadilishwa na mapadre. Hii ni bahati yenu ya kuwa Mungu anataka mwokoke, ndio maana hiyana za hao jamaa bado zinaonekana mpaka sasa. Mkipuuza, juweni baadaye watoto wenu watashindwa kuona bishara hizo, maana zitafutwa zote. Basi watakapo potea mtakuwa mmewapoteza ninyi, nao watarejesha lawama kwenu mbele ya Allah kwa dhambi hii.

Tumeeleza bishara chache za Taurati na Vitabu vingine vya Agano la Kale na Injili zenye kumhusu Mtume Muhammad *s.a.w.* ili kuhakikisha maneno ya Qur'an iliyodai kwamba Mtume *s.a.w.* ameandikwa katika Taurati na Injili. Hivyo, ni njia kubwa ya wamchao Mungu kuongoka na kushika dini ya haki. Padre Dale alikosa kabisa aliposema, Vitabu vyao "havina sifa za Muhammad" (Tafsiri yake ya Qur'an, dibaji, uk. xiv), bali hakika ni kuwa bishara nyingi na sifa za Mtume Muhammad *s.a.w.* zinapatikana katika vitabu vyao, jinsi tulivyohakikisha juu; nanyi mnatakiwa kufanya haraka kukubali dini ya Kiislamu iliyoletwa na Mtume Muhammad *s.a.w.*

Na huwaondolea mizigo yao na minyororo. Yaani,mafundisho ya Kiislamu yamenyooka sana hata yanamfungua mtu kila kamba na pingu za mila, ushirikina na ada za watu, na mtu anakuwa hana taabu ya kushikamana na desturi zisizo na maana. Wakristo wangeshika Uislamu wangeweza kufunguliwa minyororo ya dhambi ya asili na ushirikina wa namna nyingi.

Aya 159. Aya hii inaonyesha madai ya namna ya pekee ambayo hajapata kuyatamka Nabii ye yote kabla ya Mtume *s.a.w.* Hapa Mtume *s.a.w.* anaambiwa atangaze kuwa yeye ni Mtume kwa watu wote wa dunia.

وَالْاَرْضِ ۚ لَآ اِلٰهَ اِلَّا هُوَ يُحْيٖ وَيُمِيْتُ ۖ
فَاٰمِنُوْا بِاللّٰهِ وَرَسُوْلِهِ النَّبِيِّ الْاُمِّيِّ الَّذِيْ
يُؤْمِنُ بِاللّٰهِ وَكَلِمٰتِهٖ وَاتَّبِعُوْهُ لَعَلَّكُمْ
تَهْتَدُوْنَ ﴿١٥٨﴾

Ahuishaye na Afishaye. Basi Muaminini Allah na Mtume Wake, aliye Nabii Ummi, ambaye humwamini Allah na maneno Yake; na mfuateni yeye ili mpate kuongoka.

وَمِنْ قَوْمِ مُوْسٰٓى اُمَّةٌ يَّهْدُوْنَ بِالْحَقِّ
وَبِهٖ يَعْدِلُوْنَ ﴿١٥٩﴾

160. Na katika kaumu ya Musa wako watu wanaoongoza kwa haki na papo hapo wakifanya uadilifu.

وَقَطَّعْنٰهُمُ اثْنَتَيْ عَشْرَةَ اَسْبَاطًا اُمَمًا ۭ
وَاَوْحَيْنَآ اِلٰى مُوْسٰٓى اِذِ اسْتَسْقٰىهُ
قَوْمُهٗٓ اَنِ اضْرِبْ بِّعَصَاكَ الْحَجَرَ ۚ
فَانْۢبَجَسَتْ مِنْهُ اثْنَتَا عَشْرَةَ عَيْنًا ۭ قَدْ
عَلِمَ كُلُّ اُنَاسٍ مَّشْرَبَهُمْ ۭ وَظَلَّلْنَا عَلَيْهِمُ
الْغَمَامَ وَاَنْزَلْنَا عَلَيْهِمُ الْمَنَّ وَالسَّلْوٰى ۭ
كُلُوْا مِنْ طَيِّبٰتِ مَا رَزَقْنٰكُمْ ۭ وَمَا
ظَلَمُوْنَا وَلٰكِنْ كَانُوْٓا اَنْفُسَهُمْ
يَظْلِمُوْنَ ﴿١٦٠﴾

161. Na Tukawagawanya katika makabila kumi na mbili, mataifa mbalimbali. Na Tukamfunulia Musa, walipomwomba maji watu wake: Piga jiwe kwa fimbo yako; mara zikabubujika chemchem kumi na mbili na kila watu wakajua mahali pao pa kunywea. Na Tukawafunika kwa mawingu na kuwateremshia manna na salwa. Kuleni katika vitu vizuri Tulivyowapeni. Wala hawakutudhulumu Sisi, bali walikuwa wamejidhulumu wenyewe.

وَاِذْ قِيْلَ لَهُمُ اسْكُنُوْا هٰذِهِ الْقَرْيَةَ وَكُلُوْا
مِنْهَا حَيْثُ شِئْتُمْ وَقُوْلُوْا حِطَّةٌ وَّادْخُلُوا
الْبَابَ سُجَّدًا نَّغْفِرْ لَكُمْ خَطِيْۗـَٔتِكُمْ ۭ
سَنَزِيْدُ الْمُحْسِنِيْنَ ﴿١٦١﴾

162. Na walipoambiwa: Kaeni katika mji huu na humo kuleni po pote mpendapo, na semeni, Tufutie dhambi zetu; na ingieni mlangoni kwa unyenyekevu; Tutawasameheni makosa yenu; hivi karibuni Tutawazidishia watendao mema.

فَبَدَّلَ الَّذِيْنَ ظَلَمُوْا مِنْهُمْ قَوْلًا غَيْرَ
الَّذِيْ قِيْلَ لَهُمْ فَاَرْسَلْنَا عَلَيْهِمْ رِجْزًا
مِّنَ السَّمَاۗءِ بِمَا كَانُوْا يَظْلِمُوْنَ ﴿١٦٢﴾

163. Lakini wale waliodhulumu miongoni mwao wakabadilisha kauli ghairi ya ile waliyoambiwa. Basi Tukawapelekea adhabu kutoka mbinguni kwa sababu walikuwa wamedhulumu.

FUNGU 21

وَسْـَٔلْهُمْ عَنِ الْقَرْيَةِ الَّتِيْ كَانَتْ حَاضِرَةَ الْبَحْرِ ۘ اِذْ يَعْدُوْنَ فِي السَّبْتِ اِذْ تَاْتِيْهِمْ حِيْتَانُهُمْ يَوْمَ سَبْتِهِمْ شُرَّعًا وَّيَوْمَ لَا يَسْبِتُوْنَ ۙ لَا تَاْتِيْهِمْ ۚ كَذٰلِكَ ۛ نَبْلُوْهُمْ ۢ بِمَا كَانُوْا يَفْسُقُوْنَ ﴿١٦٣﴾

164. Na waulize habari za mji ambao ulikuwa kando ya bahari; (watu wa mji huo) walipokuwa wakivunja sheria ya Sabato, samaki wao walipowajia juu juu siku ya Sabato yao, na siku wasiyofanya Sabato hawakuwajia. Hivyo Tuliwajaribu kwa sababu walikuwa wakiasi.

وَاِذْ قَالَتْ اُمَّةٌ مِّنْهُمْ لِمَ تَعِظُوْنَ قَوْمًا ۙ اللّٰهُ مُهْلِكُهُمْ اَوْ مُعَذِّبُهُمْ عَذَابًا شَدِيْدًا ؕ قَالُوْا مَعْذِرَةً اِلٰى رَبِّكُمْ وَلَعَلَّهُمْ يَتَّقُوْنَ ﴿١٦٤﴾

165. Na baadhi ya watu kati yao waliposema: Kwa nini mnawaonya watu ambao Allah Atawaangamiza au kuwaadhibu kwa adhabu kali? Wakasema tupate kuwa na udhuru mbele ya Mola wetu, na huenda wakaogopa.

فَلَمَّا نَسُوْا مَا ذُكِّرُوْا بِهٖۤ اَنْجَيْنَا الَّذِيْنَ يَنْهَوْنَ عَنِ السُّوْٓءِ وَاَخَذْنَا الَّذِيْنَ ظَلَمُوْا بِعَذَابٍۭ بَـِٔيْسٍۢ بِمَا كَانُوْا يَفْسُقُوْنَ ﴿١٦٥﴾

166. Basi waliposahau waliyokumbushwa, Tukawaokoa wale waliokuwa wakikataza maovu, na Tukawakamata wale waliodhulumu kwa adhabu mbaya kwa sababu walikuwa wakiasi.

فَلَمَّا عَتَوْا عَنْ مَّا نُهُوْا عَنْهُ قُلْنَا لَهُمْ كُوْنُوْا قِرَدَةً خٰسِـِٕيْنَ ﴿١٦٦﴾

167. Na walipokataa kuyaacha waliyokatazwa, Tukawaambia: Kuweni manyani wadhalilifu.

وَاِذْ تَاَذَّنَ رَبُّكَ لَيَبْعَثَنَّ عَلَيْهِمْ اِلٰى يَوْمِ الْقِيٰمَةِ مَنْ يَّسُوْمُهُمْ سُوْٓءَ الْعَذَابِ ؕ اِنَّ رَبَّكَ لَسَرِيْعُ الْعِقَابِ ۚ وَاِنَّهٗ لَغَفُوْرٌ رَّحِيْمٌ ﴿١٦٧﴾

168. Na (kumbuka) Alipotangaza Mola wako (ya kwamba) hakika Yeye Atawapelekea mpaka siku ya Kiyama ambao watawaadhibu kwa adhabu mbaya. Hakika Mola wako ni Mwepesi wa kuadhibu, na bila shaka Yeye ni Msamehevu, Mrehemevu.

Aya 164. *Habari za mji.* Mji unaosemwa katika Aya hii unaitwa Aila (Elath), ulio kando ya bahari ya Sham. Pia umetajwa katika 1 Wafalme 7:26 na 2 Mambo ya Nyakati 8:17. Katika zama za Nabii Sulemani mji huo uliingia katika milki za Waisraeli, lakini baadaye yumkini wakaunyang'anywa. Baadaye Uzziah akaushinda, lakini ulipokuwa na Ahaz ukawatoka tena (Enc. Bib. na Jew. Enc.)

وَقَطَّعْنٰهُمْ فِي الْاَرْضِ اُمَمًا ۚ مِنْهُمُ الصّٰلِحُوْنَ وَمِنْهُمْ دُوْنَ ذٰلِكَ ۫ وَبَلَوْنٰهُمْ بِالْحَسَنٰتِ وَالسَّيِّاٰتِ لَعَلَّهُمْ يَرْجِعُوْنَ ﴿١٦٩﴾

169. Na Tukawafarikisha katika ardhi makundi makundi. Wako baadhi yao watu wema, na wengine wao kinyume cha hao. Tukawajaribu kwa mema na mabaya ili wapate kurejea.

فَخَلَفَ مِنْۢ بَعْدِهِمْ خَلْفٌ وَّرِثُوا الْكِتٰبَ يَاْخُذُوْنَ عَرَضَ هٰذَا الْاَدْنٰى وَيَقُوْلُوْنَ سَيُغْفَرُ لَنَا ۚ وَاِنْ يَّاْتِهِمْ عَرَضٌ مِّثْلُهٗ يَاْخُذُوْهُ ؕ اَلَمْ يُؤْخَذْ عَلَيْهِمْ مِّيْثَاقُ الْكِتٰبِ اَنْ لَّا يَقُوْلُوْا عَلَى اللّٰهِ اِلَّا الْحَقَّ وَدَرَسُوْا مَا فِيْهِ ؕ وَالدَّارُ الْاٰخِرَةُ خَيْرٌ لِّلَّذِيْنَ يَتَّقُوْنَ ؕ اَفَلَا تَعْقِلُوْنَ ﴿١٧٠﴾

170. Basi wakawaandamia nyuma yao kizazi kibaya waliorithi Kitabu. Wanachukua vitu vya (dunia) hii ya karibu, na wanasema: Kwa hakika tutasamehewa. Na kama vitu vingine vya namna hii vikiwafikia pia watavichukua. Je, hawakufanyiwa ahadi katika Kitabu ya kwamba hawatasema juu ya Allah ila haki? Nao wamekwisha soma yaliyomo humo; na nyumba ya Akhera ni bora kwa wale wanaoogopa; je, hamfahamu?

وَالَّذِيْنَ يُمَسِّكُوْنَ بِالْكِتٰبِ وَاَقَامُوا الصَّلٰوةَ ؕ اِنَّا لَا نُضِيْعُ اَجْرَ الْمُصْلِحِيْنَ ﴿١٧١﴾

171. Na wale wanaoshika Kitabu na wanasimamisha Sala, hakika Sisi Hatupotezi malipo ya wafanyao wema.

وَاِذْ نَتَقْنَا الْجَبَلَ فَوْقَهُمْ كَاَنَّهٗ ظُلَّةٌ وَّظَنُّوْٓا اَنَّهٗ وَاقِعٌۢ بِهِمْ ۚ خُذُوْا مَآ اٰتَيْنٰكُمْ بِقُوَّةٍ وَّاذْكُرُوْا مَا فِيْهِ لَعَلَّكُمْ تَتَّقُوْنَ ﴿١٧٢﴾ ع

172. Na Tulipoufanya mlima uwainamie kana kwamba ni kipaa na wakadhani ya kwamba utawaangukia: Shikeni kwa nguvu (hayo) Tuliyowapeni na yakumbukeni yaliyomo ili mpate kuogopa.

FUNGU 22

وَاِذْ اَخَذَ رَبُّكَ مِنْۢ بَنِيْٓ اٰدَمَ مِنْ ظُهُوْرِهِمْ ذُرِّيَّتَهُمْ وَاَشْهَدَهُمْ عَلٰٓى اَنْفُسِهِمْ ۚ اَلَسْتُ بِرَبِّكُمْ ؕ قَالُوْا بَلٰى ۛ شَهِدْنَا ۛ اَنْ تَقُوْلُوْا يَوْمَ الْقِيٰمَةِ اِنَّا كُنَّا عَنْ هٰذَا غٰفِلِيْنَ ﴿١٧٣﴾

173. Na (kumbuka) Mola wako Alipowaleta katika wanadamu kutoka migongoni mwao wazao wao, na Akawashuhudisha juu ya nafsi zao: Je Mimi si Mola wenu? Wakasema: Naam, twashuhudia. Msije mkasema siku ya Kiyama, hakika sisi tulikuwa tumeghafilika nayo.

اَوْ تَقُوْلُوْٓا اِنَّمَآ اَشْرَكَ اٰبَآؤُنَا مِنْ قَبْلُ وَكُنَّا ذُرِّيَّةً مِّنْۢ بَعْدِهِمْ ۚ اَفَتُهْلِكُنَا بِمَا فَعَلَ الْمُبْطِلُوْنَ ﴿۱۷۴﴾

174. Au mkasema, Baba zetu ndio walioshirikisha zamani, nasi tulikuwa wazao nyuma yao, je, Utatuangamiza kwa sababu ya yale waliyofanya wa-ongo?

وَكَذٰلِكَ نُفَصِّلُ الْاٰيٰتِ وَلَعَلَّهُمْ يَرْجِعُوْنَ ﴿۱۷۵﴾

175. Na hivi ndivyo Tuelezavyo Ishara, na huenda watarejea.

وَاتْلُ عَلَيْهِمْ نَبَاَ الَّذِيْٓ اٰتَيْنٰهُ اٰيٰتِنَا فَانْسَلَخَ مِنْهَا فَاَتْبَعَهُ الشَّيْطٰنُ فَكَانَ مِنَ الْغٰوِيْنَ ﴿۱۷۶﴾

176. Na wasomee habari za yule Tuliyempa Ishara Zetu, kisha akajivuna nazo, na Shetani akamfuata na akawa miongoni mwa waliopotea.

وَلَوْ شِئْنَا لَرَفَعْنٰهُ بِهَا وَلٰكِنَّهٗٓ اَخْلَدَ اِلَى الْاَرْضِ وَاتَّبَعَ هَوٰىهُ ۚ فَمَثَلُهٗ كَمَثَلِ الْكَلْبِ ۚ اِنْ تَحْمِلْ عَلَيْهِ يَلْهَثْ اَوْ تَتْرُكْهُ يَلْهَثْ ؕ ذٰلِكَ مَثَلُ الْقَوْمِ الَّذِيْنَ كَذَّبُوْا بِاٰيٰتِنَا ۚ فَاقْصُصِ الْقَصَصَ لَعَلَّهُمْ يَتَفَكَّرُوْنَ ﴿۱۷۷﴾

177. Na kama Tungalitaka Tungalimnyanyua kwazo, lakini yeye akagandamana kwenye ardhi na kuyafuata matamanio yake. Basi hali yake ni kama hali ya mbwa; ukimpiga hutweta au ukimwacha pia hutweta. Hiyo ndiyo hali ya watu waliozikadhibisha Aya Zetu. Basi simulia hadithi huenda watafikiri.

سَآءَ مَثَلًا ۨ الْقَوْمُ الَّذِيْنَ كَذَّبُوْا بِاٰيٰتِنَا وَاَنْفُسَهُمْ كَانُوْا يَظْلِمُوْنَ ﴿۱۷۸﴾

178. Ni mbaya hali ya watu wanaozikadhibisha Aya Zetu na wanajidhulumu nafsi zao wenyewe.

مَنْ يَّهْدِ اللّٰهُ فَهُوَ الْمُهْتَدِيْ ۚ وَمَنْ يُّضْلِلْ فَاُولٰٓئِكَ هُمُ الْخٰسِرُوْنَ ﴿۱۷۹﴾

179. Allah Atakayemwongoza, basi yeye ndiye aongokaye; na Atakayemhukumu kupotea, basi hao ndio wapatao hasara.

وَلَقَدْ ذَرَاْنَا لِجَهَنَّمَ كَثِيْرًا مِّنَ الْجِنِّ وَالْاِنْسِ ۖ لَهُمْ قُلُوْبٌ لَّا يَفْقَهُوْنَ بِهَا ۫ وَلَهُمْ اَعْيُنٌ لَّا يُبْصِرُوْنَ بِهَا ۫ وَلَهُمْ

180. Na bila shaka Tumewaumba wengi wa watu na majinni ambao mwisho wao ni Jahanamu! Mioyo wanayo lakini hawafahamu kwayo, na macho wanayo lakini hawaoni kwayo,

Aya 176. Aya hii haimhusu mtu ye yote maalumu; bali inawahusu watu wanaoonyeshwa Ishara na Allah kisha wakazikataa. Aya kama hii, kwa mfano pia imetokea katika sura 2:18. Aya hii watu wameihusisha kwa Bal'am bin Ba'ura, ambaye, inasimuliwa, alikuwa katika siku za Nabii Musa. Inasemekana alikuwa mtu mtawa, lakini kiburi kikamharibu na akafa katika hali ya kufedheheka. Lakini Aya hii pia inaeleza hali ya Abu Jahal, ambaye alikiri ukweli wa Mtume *s.a.w.*, lakini hakukubali kumfuata, akisema kwa dharau ya kuwa ukoo wake haujapata kuutii ukoo wa Abdu Manaf, aliyekuwa babu mkuu wa Mtume *s.a.w.*

اِذَا نَّ لَّا يَسْمَعُوْنَ بِهَا ؕ اُولٰٓئِكَ كَالْاَنْعَامِ
بَلْ هُمْ اَضَلُّ ؕ اُولٰٓئِكَ هُمُ الْغٰفِلُوْنَ ﴿۱۷۹﴾

na masikio wanayo lakini hawasikii kwayo. Hao ni kama wanyama, bali wao ni wapotevu zaidi. Hao ndio walioghafilika.

وَلِلّٰهِ الْاَسْمَآءُ الْحُسْنٰى فَادْعُوْهُ بِهَا ۪
وَذَرُوا الَّذِيْنَ يُلْحِدُوْنَ فِيْٓ اَسْمَآئِهٖ ؕ
سَيُجْزَوْنَ مَا كَانُوْا يَعْمَلُوْنَ ﴿۱۸۰﴾

181. Na Allah ndiye Mwenye majina mazuri; basi Mwombeni kwayo. Na waacheni wale wanaoharibu utakatifu wa majina Yake. Hivi karibuni watalipwa yale waliyokuwa wakiyatenda.

وَمِمَّنْ خَلَقْنَآ اُمَّةٌ يَّهْدُوْنَ بِالْحَقِّ وَبِهٖ
يَعْدِلُوْنَ ﴿۱۸۱﴾ ع ۱۳

182. Na katika wale Tuliowaumba wako watu wanaoongoza kwa haki na kwayo wanafanya uadilifu.

FUNGU 23

وَالَّذِيْنَ كَذَّبُوْا بِاٰيٰتِنَا سَنَسْتَدْرِجُهُمْ
مِّنْ حَيْثُ لَا يَعْلَمُوْنَ ﴿۱۸۲﴾ ۚ

183. Na wale waliokadhibisha Ishara Zetu, Tutawavuta kidogo kidogo kwa mahali wasipopajua.

وَاُمْلِيْ لَهُمْ ؕ اِنَّ كَيْدِيْ مَتِيْنٌ ﴿۱۸۳﴾

184. Nami Nitawapa muda; hakika mpango wangu ni madhubuti.

اَوَلَمْ يَتَفَكَّرُوْا ۗ مَا بِصَاحِبِهِمْ مِّنْ
جِنَّةٍ ؕ اِنْ هُوَ اِلَّا نَذِيْرٌ مُّبِيْنٌ ﴿۱۸۴﴾

185. Je, hawatafakari? Sahibu yao hana wehu. Siye ila ni mwonyaji dhahiri.

اَوَلَمْ يَنْظُرُوْا فِيْ مَلَكُوْتِ السَّمٰوٰتِ
وَالْاَرْضِ وَمَا خَلَقَ اللّٰهُ مِنْ شَيْءٍ ۙ وَّاَنْ
عَسٰٓى اَنْ يَّكُوْنَ قَدِ اقْتَرَبَ اَجَلُهُمْ ۚ
فَبِاَيِّ حَدِيْثٍ بَعْدَهٗ يُؤْمِنُوْنَ ﴿۱۸۵﴾

186. Je, hawaoni ufalme wa mbingu na ardhi na vitu Alivyoviumba Allah? Na inaweza kuwa ajali yao i karibu; basi baada ya haya hadithi gani watakayoiamini?

مَنْ يُّضْلِلِ اللّٰهُ فَلَا هَادِيَ لَهٗ ؕ وَيَذَرُهُمْ
فِيْ طُغْيَانِهِمْ يَعْمَهُوْنَ ﴿۱۸۶﴾

187. Ambaye Allah Anamhukumu kupotea, basi yeye hana mwongozi. Na Anawaacha katika uasi wao wakitangatanga ovyo.

Aya 181. *Majina mazuri.* Jina hasa la Allah ni Allah; mengine yote ni sifa Zake ambazo pia zinaitwa majina. Aya hi inatuambia siri ambayo kwayo maombi yetu yanaweza kupokelewa upesi. Tunapoomba tutaje sifa za Allah zinazohusiana na haja zetu.

يَسْـَٔلُوْنَكَ عَنِ السَّاعَةِ اَيَّانَ مُرْسٰىهَا ؕ قُلْ
اِنَّمَا عِلْمُهَا عِنْدَ رَبِّيْ ۚ لَا يُجَلِّيْهَا
لِوَقْتِهَاۤ اِلَّا هُوَ ۚ ثَقُلَتْ فِي السَّمٰوٰتِ
وَالْاَرْضِ ؕ لَا تَاْتِيْكُمْ اِلَّا بَغْتَةً ؕ
يَسْـَٔلُوْنَكَ كَاَنَّكَ حَفِيٌّ عَنْهَا ؕ قُلْ اِنَّمَا
عِلْمُهَا عِنْدَ اللّٰهِ وَلٰكِنَّ اَكْثَرَ النَّاسِ
لَا يَعْلَمُوْنَ ﴿۱۸۸﴾

188. Wanakuuliza juu ya saa ile: Kutokea kwake kutakuwa lini. Sema: Elimu yake iko kwa Mola wangu tu. Hakuna wa kuidhihirisha kwa wakati wake ila Yeye tu. Ni nzito katika mbingu na ardhi. Haitawafikieni ila kwa ghafla. Wanakuuliza kana kwamba wewe unajua kila kitu kuhusiana nayo. Sema: Elimu yake iko kwa Allah tu; lakini watu wengi hawajui.

قُلْ لَّاۤ اَمْلِكُ لِنَفْسِيْ نَفْعًا وَّلَا ضَرًّا
اِلَّا مَا شَآءَ اللّٰهُ ؕ وَلَوْ كُنْتُ اَعْلَمُ
الْغَيْبَ لَاسْتَكْثَرْتُ مِنَ الْخَيْرِ ۛۚ وَمَا
مَسَّنِيَ السُّوْٓءُ ؕ اِنْ اَنَا اِلَّا نَذِيْرٌ وَّبَشِيْرٌ
لِّقَوْمٍ يُّؤْمِنُوْنَ ﴿۱۸۹﴾

189. Sema: Sina mamlaka ya kujifaidia wala kujidhuru ila Apendavyo Allah; na lau kama ningaliijua ghaibu ningejizidishia heri nyingi, wala isingalinigusa dhara; mimi si cho chote ila ni Mwonyaji na Mtoaji wa habari njema kwa watu wanaoamini.

FUNGU 24

هُوَ الَّذِيْ خَلَقَكُمْ مِّنْ نَّفْسٍ وَّاحِدَةٍ
وَّجَعَلَ مِنْهَا زَوْجَهَا لِيَسْكُنَ اِلَيْهَا ۚ فَلَمَّا
تَغَشّٰىهَا حَمَلَتْ حَمْلًا خَفِيْفًا فَمَرَّتْ بِهٖ ۚ
فَلَمَّاۤ اَثْقَلَتْ دَّعَوَا اللّٰهَ رَبَّهُمَا لَئِنْ اٰتَيْتَنَا
صَالِحًا لَّنَكُوْنَنَّ مِنَ الشّٰكِرِيْنَ ﴿۱۹۰﴾

190. Yeye ndiye Aliyewaumbeni katika nafsi moja na toka hiyo Amejaalia mwenzake ili apate utulivu kwake. Na anapomjua, anabeba himila nyepesi na kutembea nayo, basi alipokuwa mzito wote wawili wakamwomba Allah, Mola wao: Kama ukitupa (mtoto) mwema, bila shaka sisi tutakuwa miongoni mwa wanaoshukuru.

فَلَمَّاۤ اٰتٰىهُمَا صَالِحًا جَعَلَا لَهٗ شُرَكَآءَ فِيْمَاۤ
اٰتٰىهُمَا ۚ فَتَعٰلَى اللّٰهُ عَمَّا يُشْرِكُوْنَ ﴿۱۹۱﴾

191. Basi Anapowapa (mtoto) mwema, wanamwekea washirika katika kile Alichowapa. Lakini Allah ni juu sana kuliko wale wanaowashirikisha.

اَيُشْرِكُوْنَ مَا لَا يَخْلُقُ شَيْـًٔا وَّهُمْ
يُخْلَقُوْنَ ﴿۱۹۲﴾

192. Je, wanawashirikisha wale ambao hawaumbi kitu hali wao wameumbwa?

Aya 188. *Saa ile,* yaani, saa ya maangamio ya makafiri.

وَلَا يَسْتَطِيْعُوْنَ لَهُمْ نَصْرًا وَّ لَآ اَنْفُسَهُمْ يَنْصُرُوْنَ ﴿۱۹۳﴾

193. Wala hawawezi kuwasaidia, wala hawawezi kujisaidia wenyewe.

وَ اِنْ تَدْعُوْهُمْ اِلَى الْهُدٰى لَا يَتَّبِعُوْكُمْ ؕ سَوَآءٌ عَلَيْكُمْ اَدَعَوْتُمُوْهُمْ اَمْ اَنْتُمْ صَامِتُوْنَ ﴿۱۹۴﴾

194. Na kama mkiwaita kwenye mwongozo hawatawafuateni. Ni mamoja kwenu ikiwa mtawaita au mtanyamaza kimya.

اِنَّ الَّذِيْنَ تَدْعُوْنَ مِنْ دُوْنِ اللّٰهِ عِبَادٌ اَمْثَالُكُمْ فَادْعُوْهُمْ فَلْيَسْتَجِيْبُوْا لَكُمْ اِنْ كُنْتُمْ صٰدِقِيْنَ ﴿۱۹۵﴾

195. Hakika wale mnaowaita badala ya Allah ni watumishi kama ninyi, basi waiteni nao wawaitikieni ikiwa ninyi mnasema kweli.

اَلَهُمْ اَرْجُلٌ يَّمْشُوْنَ بِهَآ اَمْ لَهُمْ اَيْدٍ يَّبْطِشُوْنَ بِهَآ اَمْ لَهُمْ اَعْيُنٌ يُّبْصِرُوْنَ بِهَآ اَمْ لَهُمْ اٰذَانٌ يَّسْمَعُوْنَ بِهَا ؕ قُلِ ادْعُوْا شُرَكَآءَكُمْ ثُمَّ كِيْدُوْنِ فَلَا تُنْظِرُوْنِ ﴿۱۹۶﴾

196. Je, wanayo miguu ya kuendea? Au je, wanayo mikono ya kushikia? Au je, wanayo macho ya kuonea? Au je, wanayo masikio ya kusikilia? Sema: Waiteni washirika wenu kisha shindaneni nami wala msinipe nafasi!

اِنَّ وَلِيِّۦَ اللّٰهُ الَّذِيْ نَزَّلَ الْكِتٰبَ ۖ وَهُوَ يَتَوَلَّى الصّٰلِحِيْنَ ﴿۱۹۷﴾

197. Bila shaka Mlinzi wangu ni Allah Aliyeteremsha Kitabu, naye ndiye Awalindaye wafanyao mema.

وَالَّذِيْنَ تَدْعُوْنَ مِنْ دُوْنِهٖ لَا يَسْتَطِيْعُوْنَ نَصْرَكُمْ وَلَآ اَنْفُسَهُمْ يَنْصُرُوْنَ ﴿۱۹۸﴾

198. Na wale mnaowaita badala Yake hawana uwezo wa kuwanusuruni wala kujinusuru wenyewe.

وَاِنْ تَدْعُوْهُمْ اِلَى الْهُدٰى لَا يَسْمَعُوْا ؕ وَتَرٰىهُمْ يَنْظُرُوْنَ اِلَيْكَ وَهُمْ لَا يُبْصِرُوْنَ ﴿۱۹۹﴾

199. Na kama mkiwaita kwenye mwongozo hawasikii; na unawaona wanakutazama lakini hawaoni.

خُذِ الْعَفْوَ وَاْمُرْ بِالْعُرْفِ وَاَعْرِضْ عَنِ الْجٰهِلِيْنَ ﴿۲۰۰﴾

200. Ushike usamehevu na uamrishe yaliyo mema na ujitenge na wajinga.

وَاِمَّا يَنْزَغَنَّكَ مِنَ الشَّيْطٰنِ نَزْغٌ فَاسْتَعِذْ بِاللّٰهِ ؕ اِنَّهٗ سَمِيْعٌ عَلِيْمٌ ﴿۲۰۰﴾

201. Na kama wasiwasi wa Shetani ukikusumbua, basi jikinge kwa Allah; bila shaka Yeye ndiye Asikiaye, Ajuaye.

Aya 200. Tazama uzuri wa mafundisho ya Kiislamu! Islam ingawa imezungukwa na maadui wanaotaka kuiangamiza, lakini haiachi mwendo wake wa kuvumiliana na huruma.

اِنَّ الَّذِيْنَ اتَّقَوْا اِذَا مَسَّهُمْ طٰٓئِفٌ مِّنَ الشَّيْطٰنِ تَذَكَّرُوْا فَاِذَا هُمْ مُّبْصِرُوْنَ ﴿٢٠٢﴾

202. Hakika wale wanaoogopa yanapowagusa mapatilizo ya Shetani wanamkumbuka sana (Allah), mara wanakuwa wenye busara.

وَاِخْوَانُهُمْ يَمُدُّوْنَهُمْ فِى الْغَيِّ ثُمَّ لَا يُقْصِرُوْنَ ﴿٢٠٣﴾

203. Na ndugu zao wanawavutia kwenye upotevu tena hawaziachi (juhudi hizo).

وَاِذَا لَمْ تَاْتِهِمْ بِاٰيَةٍ قَالُوْا لَوْ لَا اجْتَبَيْتَهَا ؕ قُلْ اِنَّمَآ اَتَّبِعُ مَا يُوْحٰٓى اِلَىَّ مِنْ رَّبِّىْ ۚ هٰذَا بَصَآئِرُ مِنْ رَّبِّكُمْ وَهُدًى وَّرَحْمَةٌ لِّقَوْمٍ يُّؤْمِنُوْنَ ﴿٢٠٤﴾

204. Na usipowaletea Ishara, husema: Kwa nini hukuichagua? Sema: Hakika nayafuata yaliyofunuliwa kwangu kutoka kwa Mola wangu. Hizi ni dalili zitokazo kwa Mola wenu na ni mwongozo na rehema kwa watu wanaoamini.

وَاِذَا قُرِئَ الْقُرْاٰنُ فَاسْتَمِعُوْا لَهٗ وَاَنْصِتُوْا لَعَلَّكُمْ تُرْحَمُوْنَ ﴿٢٠٥﴾

205. Na Qur'an isomwapo, basi isikilizeni na nyamazeni ili mpate kurehemiwa.

وَاذْكُرْ رَّبَّكَ فِىْ نَفْسِكَ تَضَرُّعًا وَّخِيْفَةً وَّدُوْنَ الْجَهْرِ مِنَ الْقَوْلِ بِالْغُدُوِّ وَالْاٰصَالِ وَلَا تَكُنْ مِّنَ الْغٰفِلِيْنَ ﴿٢٠٦﴾

206. Na umkumbuke Mola wako rohoni mwako kwa unyenyekevu na hofu na bila ya kupiga kelele katika usemi, asubuhi na jioni; wala usiwe miongoni mwa wenye kughafilika.

اِنَّ الَّذِيْنَ عِنْدَ رَبِّكَ لَا يَسْتَكْبِرُوْنَ عَنْ عِبَادَتِهٖ وَيُسَبِّحُوْنَهٗ وَلَهٗ يَسْجُدُوْنَ ﴿٢٠٧﴾ ۩

207. Kwa yakini wale walio karibu na Mola wako hawajivuni katika ibada Yake na wanamtukuza Yeye na kumsujudia.

Aya 206. Ingawa Islam inaruhusu maombi ya sauti kubwa na ya siri, lakini hapa maombi ya siri yanatiliwa mkazo ili yaingize moyoni unyenyekevu, uaminifu na hofu.

سُوْرَةُ الْاَنْفَالِ مَدَنِيَّةٌ وَّ هِيَ مَعَ الْبَسْمَلَةِ سِتٌّ وَّ سَبْعُوْنَ اٰيَةً وَّ عَشَرَةُ رُكُوْعَاتٍ

8. SURA AL-ANFAAL

Imeteremshwa Madina
Ina mafungu 10 na Aya 76 pamoja na Bismillahi

بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ ①

1. Kwa jina la Allah, Mwingi wa rehema, Mwingi wa ukarimu.

يَسْـَٔلُوْنَكَ عَنِ الْاَنْفَالِ ؕ قُلِ الْاَنْفَالُ لِلّٰهِ وَالرَّسُوْلِ ۚ فَاتَّقُوا اللّٰهَ وَاَصْلِحُوْا ذَاتَ بَيْنِكُمْ ۪ وَاَطِيْعُوا اللّٰهَ وَرَسُوْلَهٗۤ اِنْ كُنْتُمْ مُّؤْمِنِيْنَ ②

2. Wanakuuliza juu ya mali iliyotekwa. Sema: Mali iliyotekwa ni kwa ajili ya Allah na Mtume. Basi Mwogopeni Allah na suluhisheni mambo baina yenu, na Mtiini Allah na Mtume Wake ikiwa ninyi ni waaminio.

اِنَّمَا الْمُؤْمِنُوْنَ الَّذِيْنَ اِذَا ذُكِرَ اللّٰهُ وَجِلَتْ قُلُوْبُهُمْ وَاِذَا تُلِيَتْ عَلَيْهِمْ اٰيٰتُهٗ زَادَتْهُمْ اِيْمَانًا وَّعَلٰى رَبِّهِمْ يَتَوَكَّلُوْنَ ③ ۚ

3. Hakika waaminio ni wale ambao Anapotajwa Allah, mioyo yao hujaa hofu; na wanaposomewa Aya Zake zinawazidishia imani, na wanategemea juu ya Mola wao;

Sura *Anfaal* na sura *Tauba* au *Baraa-at* ni za Madina. Sura *Anfaal* iliteremshwa kama wakati wa vita vya Badri, katika mwaka wa kwanza au wa pili wa Hijra. Lakini kwa kuwa Aya saba za sura hii zimetaja hila za makafiri walizofanya wakati wa kuhama Mtume, baadhi ya wafasiri wameziona Aya hizo kama za Makka. Hili ni kosa lililo wazi, maana Qur'an kwa maneno hayo hayo imeeleza matukio katika maisha ya Adamu, Ibrahimu na Musa. Ikiwa Aya yo yote inaweza kuonekana kuwa ya Makka kwa sababu inataja jambo lililotokea Makka, je, Aya inayoelezea habari iliyotokea katika siku za Adamu au za Ibrahimu au za Musa itasemwa ilishuka katika nyakati za Mitume hao? Asemavyo Imamu Bukhari, sura *Tauba* au *Baraa-at* ilikuwa katika sehemu za mwisho za Qur'an zilizoshuka baada ya Hijra, ambapo sura *Anfaal* ilikuwa katika sehemu za kwanza kushuka baada ya Hijra.

Sura *Tauba* ni sehemu tu ya sura *Anfaal,* na kwa sababu hiyo sura *Tauba* haina Bismillahi. Neno *Anfaal* maana yake ni "Mali iliyotekwa" na neno *Tauba* maana yake ni "Toba" na *Baraa-at* maana yake ni "Tangazo la kujitoa katika dhima."

Aya 2. *Anfaal,* "Mali iliyotekwa" maana yake ni mateka au faida inayokuja kwa sura ya fadhili ya Mungu bila mtu kuishughulikia au kuistahili (Mufradat).

Aya hii haielezi habari za kugawanya mali ya mateka. Sheria ya jambo hilo iko katika sura 8:42 huko mbele. Aya hii inaeleza tu kupata mapato au mateka; siyo namna ya kuyagawanya.

الَّذِيْنَ يُقِيْمُوْنَ الصَّلٰوةَ وَ مِمَّا رَزَقْنٰهُمْ يُنْفِقُوْنَ ۝٤

4. Ambao wanasimamisha Sala na wanatoa katika yale Tuliyowapa.

اُولٰٓئِكَ هُمُ الْمُؤْمِنُوْنَ حَقًّا ؕ لَهُمْ دَرَجٰتٌ عِنْدَ رَبِّهِمْ وَمَغْفِرَةٌ وَّرِزْقٌ كَرِيْمٌ ۝٥

5. Hao ndio waaminio kweli kweli. Wao wana vyeo kwa Mola wao, na msamaha na riziki yenye heshima.

كَمَآ اَخْرَجَكَ رَبُّكَ مِنْۢ بَيْتِكَ بِالْحَقِّ ۖ وَاِنَّ فَرِيْقًا مِّنَ الْمُؤْمِنِيْنَ لَكٰرِهُوْنَ ۝٦

6. Kama Alivyokutoa Mola wako katika nyumba yako kwa haki, na hakika kundi moja la waaminio hawakupenda.

يُجَادِلُوْنَكَ فِي الْحَقِّ بَعْدَ مَا تَبَيَّنَ كَاَنَّمَا يُسَاقُوْنَ اِلَى الْمَوْتِ وَهُمْ يَنْظُرُوْنَ ۝٧

7. Wakabishana nawe katika haki baada ya kubainika (haki ile) kana kwamba wanasukumwa kwenye mauti na hali wanaona.

وَاِذْ يَعِدُكُمُ اللّٰهُ اِحْدَى الطَّآئِفَتَيْنِ اَنَّهَا لَكُمْ وَتَوَدُّوْنَ اَنَّ غَيْرَ ذَاتِ الشَّوْكَةِ تَكُوْنُ لَكُمْ وَيُرِيْدُ اللّٰهُ اَنْ يُّحِقَّ الْحَقَّ بِكَلِمٰتِهٖ وَيَقْطَعَ دَابِرَ الْكٰفِرِيْنَ ۝٨

8. Na (kumbukeni) Allah Alipowaahidini moja kati ya makundi mawili ya kwamba hilo ni lenu, nanyi mkapenda mpate lile lisilo na uwezo wa kudhuru na Allah Anapenda kuithibitisha haki kwa maneno Yake na kuikata mizizi ya makafiri.

لِيُحِقَّ الْحَقَّ وَيُبْطِلَ الْبَاطِلَ وَلَوْ كَرِهَ الْمُجْرِمُوْنَ ۝٩

9. Ili kuithibitisha haki na kuibatilisha batili, ijapokuwa wahalifu wachukie.

اِذْ تَسْتَغِيْثُوْنَ رَبَّكُمْ فَاسْتَجَابَ لَكُمْ اَنِّيْ مُمِدُّكُمْ بِاَلْفٍ مِّنَ الْمَلٰٓئِكَةِ مُرْدِفِيْنَ ۝١٠

10. (Kumbukeni) mlipokuwa mkiomba msaada kwa Mola wenu, naye Akawajibuni: Kwa yakini Mimi Nitawasaidieni kwa Malaika elfu moja wafuatanao mfululizo.

وَمَا جَعَلَهُ اللّٰهُ اِلَّا بُشْرٰى وَلِتَطْمَئِنَّ بِهٖ قُلُوْبُكُمْ ۚ وَمَا النَّصْرُ اِلَّا مِنْ عِنْدِ اللّٰهِ ؕ اِنَّ اللّٰهَ عَزِيْزٌ حَكِيْمٌ ۝١١

11. Na Allah Hakufanya haya ila iwe habari ya furaha na ili mioyo yenu itulie kwayo. Na hakuna msaada ila utokao kwa Allah; hakika Allah ni Mwenye ushindi kamili, Mwenye hekima.

Aya 6. *Kwa haki*. Kauli hii inaonyesha kuwa kutoka kwa Mtume *s.a.w.* Madina ili kukutana na adui katika vita vya Badri kulikuwa ni kwa amri ya Allah, na ya kwamba Mungu asingewaacha Waislamu kuangamizwa baada ya kuwatoa kwa amri yake.

Aya 8. *Moja katika mataifa mawili.* Makundi haya mawili ni: (1) Jeshi la watu wa Makka lililokuja kupigana na Waislamu, na (2) ni msafara wa watu wa Makka uliokuwa unarudi Makka.

Lisilo na nguvu ni ule msafara.

FUNGU 2

إِذْ يُغَشِّيكُمُ النُّعَاسَ أَمَنَةً مِّنْهُ وَيُنَزِّلُ عَلَيْكُم مِّنَ السَّمَاءِ مَاءً لِّيُطَهِّرَكُم بِهِ وَيُذْهِبَ عَنكُمْ رِجْزَ الشَّيْطَانِ وَلِيَرْبِطَ عَلَىٰ قُلُوبِكُمْ وَيُثَبِّتَ بِهِ الْأَقْدَامَ ﴿١٢﴾

12. (Kumbukeni) Alipowafunikeni kwa usingizi uliokuwa (alama ya) amani itokayo Kwake, na Akawateremshieni maji kutoka mawinguni ili kuwatakaseni kwayo na kuwaondoleeni uchafu wa Shetani na kuipa nguvu mioyo yenu na pia kwayo kuiimarisha miguu.

إِذْ يُوحِي رَبُّكَ إِلَى الْمَلَائِكَةِ أَنِّي مَعَكُمْ فَثَبِّتُوا الَّذِينَ آمَنُوا ۚ سَأُلْقِي فِي قُلُوبِ الَّذِينَ كَفَرُوا الرُّعْبَ فَاضْرِبُوا فَوْقَ الْأَعْنَاقِ وَاضْرِبُوا مِنْهُمْ كُلَّ بَنَانٍ ﴿١٣﴾

13. (Kumbukeni) Mola wako Alipowafunulia Malaika: Hakika Mimi ni pamoja nanyi, basi waimarisheni walioamini; hivi karibuni nitatia woga mioyoni mwa waliokufuru. Basi wapigeni juu ya shingo (zao) na wapigeni kwenye kila ncha za vidole.

Aya 13. Padre Dale amezoea sana kusema ya kuwa adhabu hizi ni za kishenzi (uk. 600, 572 na 580 wa Tafsiri yake). Lakini haonekani kuangalia ya kuwa hapa Waislamu wanafunzwa kuvunja jeuri ya wadhalimu wanaoleta vita na kuharibu amani. Hakuna njia ya kupigana na adui vitani aliyejifunga kuja kukuua, kwa namna ya kwamba umshinde kwa kumfanya arejee kwake bila mapigo ya kumwua au kumwumiza. Watu wanaochafua amani na kuleta taabu za bure kwa watu wema waliotulia, bila shaka wanastahili adhabu zilizo kali. Juu ya hayo, Padre Dale angeangalia kwanza mafunzo ya dini yake juu ya jambo hili. Habari za vita vya Biblia, zisome katika maelezo ya sura 22:40, nawe utaona hali yao ilivyo; wala sio wao wa kulaumu mafunzo yasiyo na hatia ya dini ya Kiislamu. Kwa mfano, soma Isaya 13:13-16 maneno haya:-

"Kwa hiyo nitazitetemesha mbingu, na dunia itatikiswa itoke katika mahali pake, kwa sababu ya ghadhabu ya BWANA wa majeshi, na kwa sababu ya siku ya hasira yake kali . . . . Kila mtu atakayeonekana atatumbuliwa, na kila mtu atakayepatikana ataanguka kwa upanga. Na watoto wao wachanga watavunjwa-vunjwa mbele ya macho yao, nyumba zao zitatekwa nyara, na wake zao watatendewa jeuri." Sasa Padre Dale anafikirije juu ya shambulio hili linaloahidiwa na Kitabu anachokiamini: la kiungwana au la kishenzi?

Ama kwa adhabu nyinginezo, soma Kitabu chao kiitwacho Mwanzo 19:24-25 maneno haya, "Ndipo BWANA akanyesha juu ya Sodoma na juu ya Gomora kiberiti cha moto toka mbinguni kwa BWANA. Akaangusha miji hiyo na Bonde lote, na wote waliokaa katika miji hiyo, na yote yaliyomea katika nchi ile." Adhabu hii nayo Padre Dale anaionaje, ya kishenzi au ya kiungwana?

Kwa Wakristo, Jahanamu ni mahali pa kuungua wakosefu milele bila kutoka (Marko 9:46). Dini ya Kiislamu inafundisha ya kuwa adhabu ya Jahanamu ni kali, haina mfano kwa ukali wake, na watu wataadhibiwa humo kwa muda mrefu sana, hata kwa karne nyingi; lakini muda wa adhabu yao ukiisha watatolewa, kama vile watokavyo wagonjwa hospitali wanapopona, na wataingizwa peponi. Jahanamu ya Kiislamu ni kama hospitali, anakotibiwa mtu maovu yake ili apone na kupata nguvu za kutosha kuziona na kuzifaidi starehe za Peponi. Kwa mfano mtu akiwa mgonjwa, chakula kizuri hukiona chapwa; hewa nzuri inayompa raha mtu mzima, yeye anatetemeka kwa baridi; kitanda laini cha godoro yeye anaona kama amelala penye miiba. Kadhalika maovu yanaitia roho ugonjwa hata haiwezi kuona raha po pote itakapowekwa. Jahanamu ndio yenye utibabu

ذٰلِكَ بِاَنَّهُمْ شَآقُّوا اللّٰهَ وَرَسُوْلَهٗ ۚ وَمَنْ يُّشَاقِقِ اللّٰهَ وَرَسُوْلَهٗ فَاِنَّ اللّٰهَ شَدِيْدُ الْعِقَابِ ﴿١٤﴾

14. Hayo ni kwa sababu wamemwasi Allah na Mtume Wake. Na mwenye kumwasi Allah na Mtume Wake, basi hakika Allah ni Mkali wa kuadhibu.

ذٰلِكُمْ فَذُوْقُوْهُ وَاَنَّ لِلْكٰفِرِيْنَ عَذَابَ النَّارِ ﴿١٥﴾

15. Ndio hayo, basi ionjeni; na bila shaka makafiri wana adhabu ya Moto.

يٰٓاَيُّهَا الَّذِيْنَ اٰمَنُوْٓا اِذَا لَقِيْتُمُ الَّذِيْنَ كَفَرُوْا زَحْفًا فَلَا تُوَلُّوْهُمُ الْاَدْبَارَ ﴿١٦﴾

16. Enyi mlioamini, mkutanapo vitani na jeshi la wale waliokufuru, basi msiwageuzie migongo.

وَمَنْ يُّوَلِّهِمْ يَوْمَئِذٍ دُبُرَهٗٓ اِلَّا مُتَحَرِّفًا لِّقِتَالٍ اَوْ مُتَحَيِّزًا اِلٰى فِئَةٍ فَقَدْ بَآءَ بِغَضَبٍ مِّنَ اللّٰهِ وَمَاْوٰىهُ جَهَنَّمُ ۭ وَبِئْسَ الْمَصِيْرُ ﴿١٧﴾

17. Na atakayewageuzia mgongo wake siku hiyo, isipokuwa amegeuka kwa kushambulia au kageuka kuungana na jeshi, basi hakika yeye amerudi na ghadhabu ya Allah, na mahali pake ni Jahanamu, napo ni mahali pabaya pa kurudia!

فَلَمْ تَقْتُلُوْهُمْ وَلٰكِنَّ اللّٰهَ قَتَلَهُمْ ۠ وَمَا رَمَيْتَ اِذْ رَمَيْتَ وَلٰكِنَّ اللّٰهَ رَمٰى ۚ وَلِيُبْلِيَ الْمُؤْمِنِيْنَ مِنْهُ بَلَآءً حَسَنًا ۭ اِنَّ اللّٰهَ سَمِيْعٌ عَلِيْمٌ ﴿١٨﴾

18. Basi ninyi hamkuwaua, lakini Allah ndiye Amewaua; na hukutupa wewe ulipotupa, walakini Allah ndiye Aliyetupa, ili Awape waaminio majaribio kutoka Kwake, majaribio mazuri, Hakika Allah Ndiye Asikiaye Ajuaye.

---

wake, lakini utibabu huo ni wa maumivu kupita kiasi, ni kuungua hasa katika moto mkali wa namna ambayo hujapata kuiona, tena kwa muda mrefu kabisa, sawa na maradhi yake ya kiroho. Anapopona basi anatiwa Peponi, maana mtu ameumbwa kwa ajili ya Pepo, na Motoni hujitia mwenyewe kwa kuvunja miiko.

Ni wazi sasa ya kuwa Jahanamu inayofundishwa na Uislamu ni sawa na haki na uadilifu. Ya Kikristo ndio inaweza kuitwa ya kishenzi, maana mtu na awe mbaya kiasi gani, hakosi wema japo mmoja. Na akose namna gani, muda wa kukosa kwake ni miaka michache tu ya umri wake wa kuwa na akili. Sasa kama ataadhibiwa milele, bila ukomo, kwa makosa yaliyokuwa na muda maalumu tu, na ule wema wake kidogo upotee bure, usilipiwe thawabu, ndio hasa uonezi, na ndio hasa adhabu ya kishenzi na ya udhalimu ambayo kusema Mungu atafanya hivyo ni dhahiri kumsingizia. Kumbe! hiyo hiyo ndio adhabu inayofundishwa na Ukristo; lakini mapadre kama Dale hujaribu kuficha ushenzi wa dini yao kwa kuulaumu bure Uislamu.

Aya 18. *Ulipotupa*. Katika vita vya Badri Mtume *s.a.w.* alichukua gao la mchanga, akaomba dua, na akawatupia maadui. Mara ilitimka tufani ya mchanga na kuwavuruga maadui wasiweze kuona, na Waislamu wakawashambulia na kuwashinda kabisa.

ذٰلِكُمْ وَاَنَّ اللّٰهَ مُوْهِنُ كَيْدِ الْكٰفِرِيْنَ ﴿١٨﴾

19. Hiyo ndio ilivyokuwa hali yenu, na hakika Allah ndiye Adhoofishaye hila za makafiri.

اِنْ تَسْتَفْتِحُوْا فَقَدْ جَآءَكُمُ الْفَتْحُ ۚ وَاِنْ تَنْتَهُوْا فَهُوَ خَيْرٌ لَّكُمْ ۚ وَاِنْ تَعُوْدُوْا نَعُدْ ۚ وَلَنْ تُغْنِيَ عَنْكُمْ فِئَتُكُمْ شَيْـًٔا وَّلَوْ كَثُرَتْ ۙ وَاَنَّ اللّٰهَ مَعَ الْمُؤْمِنِيْنَ ﴿١٩﴾

20. Kama mlikuwa mnautaka ushindi, basi ushindi umeshawafikieni, na kama mkijizuia, basi itakuwa bora kwenu; na kama mtarudia (kupigana nasi) Sisi pia Tutarudia, na jeshi lenu halitawafaeni cho chote hata likiwa na watu wengi. Na kwa hakika Allah Yu pamoja na waaminio.

FUNGU 3

يٰٓاَيُّهَا الَّذِيْنَ اٰمَنُوْٓا اَطِيْعُوا اللّٰهَ وَرَسُوْلَهٗ وَلَا تَوَلَّوْا عَنْهُ وَاَنْتُمْ تَسْمَعُوْنَ ﴿٢٠﴾

21. Enyi mlioamini, Mtiini Allah na Mtume Wake, wala msijiepushe naye na hali mnasikia.

وَلَا تَكُوْنُوْا كَالَّذِيْنَ قَالُوْا سَمِعْنَا وَهُمْ لَا يَسْمَعُوْنَ ﴿٢١﴾

22. Wala msiwe kama wale wasemao: Tumesikia na kumbe hawasikii.

اِنَّ شَرَّ الدَّوَآبِّ عِنْدَ اللّٰهِ الصُّمُّ الْبُكْمُ الَّذِيْنَ لَا يَعْقِلُوْنَ ﴿٢٢﴾

23. Hakika wanyama wabaya zaidi mbele ya Allah ni viziwi, mabubu ambao hawatumii akili.

وَلَوْ عَلِمَ اللّٰهُ فِيْهِمْ خَيْرًا لَّاَسْمَعَهُمْ ؕ وَلَوْ اَسْمَعَهُمْ لَتَوَلَّوْا وَّهُمْ مُّعْرِضُوْنَ ﴿٢٣﴾

24. Na kama Allah angalijua wema wo wote kwao, bila shaka Angewasikilizisha; na kama Angaliwasikilizisha hakika wangaligeuka wakipuuza.

يٰٓاَيُّهَا الَّذِيْنَ اٰمَنُوا اسْتَجِيْبُوْا لِلّٰهِ وَلِلرَّسُوْلِ اِذَا دَعَاكُمْ لِمَا يُحْيِيْكُمْ ۚ وَاعْلَمُوْٓا اَنَّ اللّٰهَ يَحُوْلُ بَيْنَ الْمَرْءِ وَقَلْبِهٖ وَاَنَّهٗٓ اِلَيْهِ تُحْشَرُوْنَ ﴿٢٤﴾

25. Enyi mlioamini, Mwitikieni Allah na Mtume anapowaiteni ili Akuhuisheni. Na jueni ya kwamba Allah Huingia kati ya mtu na moyo wake, na ya kwamba Kwake Yeye mtakusanywa.

Aya 25. Yatakayowapeni uzima. Hapa Mtume *s.a.w.* vile vile ameambiwa kuwa anawapa watu uhai. Lakini siyo maana yake kuwa aliwafufua watu waliokufa. Hivyo kama Qur'an inaeleza juu ya Nabii ye yote kufufua wafu au kuwapa watu uhai, mradi wake ni kutoa uhai wa kiroho.

وَاتَّقُوْا فِتْنَةً لَّا تُصِيْبَنَّ الَّذِيْنَ ظَلَمُوْا مِنْكُمْ خَآصَّةً ۚ وَاعْلَمُوْٓا اَنَّ اللّٰهَ شَدِيْدُ الْعِقَابِ ﴿٢٥﴾

26. Na iogopeni fitina ambayo haitawasibu wale peke yao waliodhulumu miongoni mwenu, na jueni ya kwamba Allah ni Mkali wa kuadhibu.

وَاذْكُرُوْٓا اِذْ اَنْتُمْ قَلِيْلٌ مُّسْتَضْعَفُوْنَ فِى الْاَرْضِ تَخَافُوْنَ اَنْ يَّتَخَطَّفَكُمُ النَّاسُ فَاٰوٰىكُمْ وَاَيَّدَكُمْ بِنَصْرِهٖ وَرَزَقَكُمْ مِّنَ الطَّيِّبٰتِ لَعَلَّكُمْ تَشْكُرُوْنَ ﴿٢٦﴾

27. Na kumbukeni mlipokuwa wachache mkionekana wadhaifu katika ardhi mkawaogopa watu kuwanyang'anyeni, lakini Yeye akawapeni makao na kuwasaidieni kwa msaada Wake na kuwapeni vitu vizuri ili mpate kushukuru.

يٰٓاَيُّهَا الَّذِيْنَ اٰمَنُوْا لَا تَخُوْنُوا اللّٰهَ وَالرَّسُوْلَ وَتَخُوْنُوْٓا اَمٰنٰتِكُمْ وَاَنْتُمْ تَعْلَمُوْنَ ﴿٢٧﴾

28. Enyi mlioamini, msimfanyie hiana Allah na Mtume waila matokeo yake mtazifanyia hiyana amana zenu na hali mnajua.

وَاعْلَمُوْٓا اَنَّمَآ اَمْوَالُكُمْ وَاَوْلَادُكُمْ فِتْنَةٌ ۙ وَّاَنَّ اللّٰهَ عِنْدَهٗٓ اَجْرٌ عَظِيْمٌ ﴿٢٨﴾ ع

29. Na jueni kwamba mali zenu na watoto wenu ni jaribio na ya kwamba kwa Allah yako malipo makuu.

FUNGU 4

يٰٓاَيُّهَا الَّذِيْنَ اٰمَنُوْٓا اِنْ تَتَّقُوا اللّٰهَ يَجْعَلْ لَّكُمْ فُرْقَانًا وَّيُكَفِّرْ عَنْكُمْ سَيِّاٰتِكُمْ وَيَغْفِرْ لَكُمْ ۗ وَاللّٰهُ ذُو الْفَضْلِ الْعَظِيْمِ ﴿٢٩﴾

30. Enyi mlioamini, mkimcha Allah Atawafanyieni alama ipambanuayo na Atawafutieni makosa yenu na kuwasameheni; na Allah ni Mwenye fadhili kuu.

وَاِذْ يَمْكُرُ بِكَ الَّذِيْنَ كَفَرُوْا لِيُثْبِتُوْكَ اَوْ يَقْتُلُوْكَ اَوْ يُخْرِجُوْكَ ۗ وَيَمْكُرُوْنَ وَيَمْكُرُ اللّٰهُ ۗ وَاللّٰهُ خَيْرُ الْمٰكِرِيْنَ ﴿٣٠﴾

31. Na (kumbuka) walipokufanyia hila wale waliokufuru ili wakufunge au wakuue au wakufukuze; na wakafanya hila; na pia Allah Akafanya mpango wa kuivunja hila yao,na Allah ni Mbora wa wafanyo mipango.

Mungu Huingia kati ya mtu na moyo wake. Yaani, mtu anaposikia habari njema azifuate upesiupesi, isije kwa kupuuza kwake Mungu auachie moyo wake kushika kutu, na asiweze kuongoka.

Aya 31. Hizi ndizo hila za kila namna zilizofanywa na maadui wa Mtume *s.a.w.* huko

وَاِذَا تُتْلٰى عَلَيْهِمْ اٰيٰتُنَا قَالُوْا قَدْ سَمِعْنَا لَوْ نَشَآءُ لَقُلْنَا مِثْلَ هٰذَآ ۙ اِنْ هٰذَآ اِلَّآ اَسَاطِيْرُ الْاَوَّلِيْنَ ﴿٣١﴾

32. Na wanaposomewa Aya Zetu, husema: Tumekwisha sikia. Tungependa bila shaka tungesema kama haya. Haya si cho chote ila ni hadithi tu za watu wa kale.

وَاِذْ قَالُوا اللّٰهُمَّ اِنْ كَانَ هٰذَا هُوَ الْحَقَّ مِنْ عِنْدِكَ فَاَمْطِرْ عَلَيْنَا حِجَارَةً مِّنَ السَّمَآءِ اَوِ ائْتِنَا بِعَذَابٍ اَلِيْمٍ ﴿٣٢﴾

33. Na (kumbuka) waliposema: Ee Allah, kama haya ni haki itokayo Kwako, basi Utupigishie mvua ya mawe kutoka mbinguni au Utuletee adhabu iumizayo.

وَمَا كَانَ اللّٰهُ لِيُعَذِّبَهُمْ وَاَنْتَ فِيْهِمْ ۚ وَمَا كَانَ اللّٰهُ مُعَذِّبَهُمْ وَهُمْ يَسْتَغْفِرُوْنَ ﴿٣٣﴾

34. Lakini Allah Hakuwa wa kuwaadhibu madhali wewe umo ndani yao, wala Allah Hakuwa wa kuwaadhibu hali wanaomba msamaha.

وَمَا لَهُمْ اَلَّا يُعَذِّبَهُمُ اللّٰهُ وَهُمْ يَصُدُّوْنَ عَنِ الْمَسْجِدِ الْحَرَامِ وَمَا كَانُوْٓا اَوْلِيَآءَهٗ ۭ اِنْ اَوْلِيَآؤُهٗٓ اِلَّا الْمُتَّقُوْنَ وَلٰكِنَّ اَكْثَرَهُمْ لَا يَعْلَمُوْنَ ﴿٣٤﴾

35. Na wana udhuru gani ili Allah Asiwaadhibu hali wanazuilia (watu) Msikiti Mtakatifu nao hawakuwa walinzi wake? Si walinzi wake isipokuwa wacha-Mungu tu, lakini wengi wao hawajui.

Makka baada ya kushauriana katika baraza yao iliyoitwa *Daarun-Nadwa.* Walitoa mashauri ya namna mbalimbali, lakini shauri moja ndilo wakalikubali ya kuwa watu wa kila ukoo waunganike kumwua Mtume. Lakini Allah Alimjulisha Mtume *s.a.w.* hila yao hii, akaweza kuwaponyoka hali wameizunguka nyumba yake usiku. Ikawa ndio safari ya moja kwa moja Mtume kuhamia Madina.

Aya 32. *Tungependa bila shaka tungesema kama haya*. Lakini maneno haya ya makafiri ni madai ya bure. Qur'an ilikwisha waambia kuwa hata kama waunganike hawawezi kutoa hata sawa na sura ndogo ya Qur'an; na kweli wameshindwa.

Aya 33. Haya ni maombi yaliyoombwa na kiongozi wa makafiri, Abu Jahal, wakati wa Badri ya kwamba kama Mtume *s.a.w*. ana haki, yeye (Abu Jahal) pamoja na watu wake, wapigwe na mvua ya mawe (Bukhari, sura *Tafsiir*). Dua yake hii ilipokelewa, na si kama yeye na wenzake tu walishukiwa na adhabu, bali pia walipigwa na mawe ya changarawe kubwa-kubwa zilizopeperushwa na tufani wakati Mtume *s.a.w* alipowatupia fumba moja la mchanga (sura 8:18).

Aya 34. Aya hii inaonyesha namna gani watu wanaweza kusalimika na adhabu ya Allah: (1) Watu hawaadhibiwi Mtume wa Mungu anapokuwa anakaa pamoja nao; (2) hawaadhibiwi wanapokuwa wanaomba msamaha kwa Allah.

وَمَا كَانَ صَلَاتُهُمْ عِنْدَ الْبَيْتِ اِلَّا مُكَآءً وَّتَصْدِيَةً ؕ فَذُوْقُوا الْعَذَابَ بِمَا كُنْتُمْ تَكْفُرُوْنَ ﴿۳۶﴾

36. Na haikuwa sala yao kwenye Nyumba ila miluzi na makofi. Basi onjeni adhabu kwa sababu ya yale mliyokuwa mkikufuru.

اِنَّ الَّذِيْنَ كَفَرُوْا يُنْفِقُوْنَ اَمْوَالَهُمْ لِيَصُدُّوْا عَنْ سَبِيْلِ اللّٰهِ ؕ فَسَيُنْفِقُوْنَهَا ثُمَّ تَكُوْنُ عَلَيْهِمْ حَسْرَةً ثُمَّ يُغْلَبُوْنَ ؕ وَالَّذِيْنَ كَفَرُوْٓا اِلٰى جَهَنَّمَ يُحْشَرُوْنَ ﴿۳۷﴾

37. Hakika wale waliokufuru hutoa mali zao ili kuzuilia (watu) njia ya Allah, na bila shaka watazitoa kisha zitakuwa majuto juu yao, kisha watashindwa. Na wale waliokufuru watakusanywa kwenye Jahanamu.

لِيَمِيْزَ اللّٰهُ الْخَبِيْثَ مِنَ الطَّيِّبِ وَيَجْعَلَ الْخَبِيْثَ بَعْضَهٗ عَلٰى بَعْضٍ فَيَرْكُمَهٗ جَمِيْعًا فَيَجْعَلَهٗ فِىْ جَهَنَّمَ ؕ اُولٰٓئِكَ هُمُ الْخٰسِرُوْنَ ﴿۳۸﴾ ع

38. Ili Allah Apate kupambanua kilicho kibaya katika kizuri, na kukiweka kibaya juu ya kibaya kingine na kuvirundika vyote pamoja na kuvitupa katika Jahanamu. Hao ndio wapatao hasara.

FUNGU 5

قُلْ لِّلَّذِيْنَ كَفَرُوْٓا اِنْ يَّنْتَهُوْا يُغْفَرْ لَهُمْ مَّا قَدْ سَلَفَ ۚ وَاِنْ يَّعُوْدُوْا فَقَدْ مَضَتْ سُنَّتُ الْاَوَّلِيْنَ ﴿۳۹﴾

39. Waambie wale waliokufuru, kama wataacha watasamehewa yaliyopita, na kama wakirudia, basi umekwisha pita mfano wa watu wa kwanza.

وَقَاتِلُوْهُمْ حَتّٰى لَا تَكُوْنَ فِتْنَةٌ وَّيَكُوْنَ الدِّيْنُ كُلُّهٗ لِلّٰهِ ۚ فَاِنِ انْتَهَوْا فَاِنَّ اللّٰهَ بِمَا يَعْمَلُوْنَ بَصِيْرٌ ﴿۴۰﴾

40. Na piganeni nao mpaka yasiweko mateso, na dini iwe kabisa kwa ajili ya Allah. Lakini wakiacha, basi hakika Allah Anayaona wanayoyatenda.

وَاِنْ تَوَلَّوْا فَاعْلَمُوْٓا اَنَّ اللّٰهَ مَوْلٰىكُمْ ؕ نِعْمَ الْمَوْلٰى وَنِعْمَ النَّصِيْرُ ﴿۴۱﴾

41. Na kama wakigeuka, basi jueni kwamba Allah ndiye Mola wenu; ni Mola Mwema na Msaidizi Mwema.

Aya 40. Aya hii inaonyesha ya kuwa mapigano ilitakiwa yaendelezwe kwa muda ule tu watu wanapokuwa wanazuiliwa kufuata dini waitakayo na wanateswa. Kama maadui wa Waislamu wanaacha kupigana, Waislamu pia wanalazimika kuacha mapigano. Dini ya Kiislamu ilipigana ili kujilinda tu na kusimamisha uhuru wa dhamiri, kila mtu awe na hiyari kushika dini yo yote aitakayo bila kusumbuliwa. Watu wanaosema dini ya Kiislamu ilienezwa kwa upanga, na watu wakasilimishwa kwa nguvu, wametunga uwongo ambao umewafedhehesha. Tazama sura 22:40.

JUZU 10

وَاعْلَمُوْٓا اَنَّمَا غَنِمْتُمْ مِّنْ شَيْءٍ فَاَنَّ لِلّٰهِ خُمُسَهٗ وَلِلرَّسُوْلِ وَلِذِي الْقُرْبٰى وَالْيَتٰمٰى وَالْمَسٰكِيْنِ وَابْنِ السَّبِيْلِ ۙ اِنْ كُنْتُمْ اٰمَنْتُمْ بِاللّٰهِ وَمَآ اَنْزَلْنَا عَلٰى عَبْدِنَا يَوْمَ الْفُرْقَانِ يَوْمَ الْتَقَى الْجَمْعٰنِ ۭ وَاللّٰهُ عَلٰي كُلِّ شَيْءٍ قَدِيْرٌ ۝۴۱

42. Na jueni ya kwamba cho chote mnachoteka, basi sehemu yake ya tano ni kwa ajili ya Allah na Mtume na jamaa na yatima na maskini na msafiri, ikiwa ninyi mmemwamini Allah na yale Tuliyoyateremsha kwa Mtumishi Wetu siku ya Kipambanuzi, siku yalipokutana majeshi mawili; Na Allah ndiye Mwenye uwezo juu ya kila kitu.

اِذْ اَنْتُمْ بِالْعُدْوَةِ الدُّنْيَا وَهُمْ بِالْعُدْوَةِ الْقُصْوٰى وَالرَّكْبُ اَسْفَلَ مِنْكُمْ ۭ وَلَوْ تَوَاعَدْتُّمْ لَاخْتَلَفْتُمْ فِي الْمِيْعٰدِ ۙ وَلٰكِنْ لِّيَقْضِيَ اللّٰهُ اَمْرًا كَانَ مَفْعُوْلًا ۙ لِّيَهْلِكَ مَنْ هَلَكَ عَنْۢ بَيِّنَةٍ وَّيَحْيٰى مَنْ حَيَّ عَنْۢ بَيِّنَةٍ ۭ وَاِنَّ اللّٰهَ لَسَمِيْعٌ عَلِيْمٌ ۝۴۲ۙ

43. (Kumbukeni) mlipokuwa upande wa karibu (wa bonde) nao walipokuwa upande wa mbali (wa bonde), na msafara ulipokuwa upande wa chini yenu; na kama mngaliwekeana ahadi (ya kupigana vita na kundi lolote lile) hata hivyo mgehitilafiana katika kuupanga (muda wake), lakini (ilitokea) kwa sababu hii, ili Allah Alitimize jambo lililokuwa lenye kutendeka; ili aangamie aangamiae kwa dalili dhahiri, na aishi aishiye kwa dalili dhahiri. Na hakika Allah ndiye Asikiaye Ajuaye.

اِذْ يُرِيْكَهُمُ اللّٰهُ فِيْ مَنَامِكَ قَلِيْلًا ۭ

44. (Kumbuka) Allah Alipokuonyesha katika usingizi wako kwamba wao ni wachache. Na kama

---

Aya 42. Aya hii (pia tazama sura 8:2) inaeleza habari za kugawanya mali za mateka. Sehemu 1/5 ya mali hiyo iwekwe kando, na inayobaki igawanyiwe askari (ambao hawakuwa wanapewa mshahara). Katika sehemu ile 1/5 Mtume alikuwa anachukua kidogo na inayobaki anawagawanyia ndugu zake na mayatima na maskini na wasafiri. Baada ya Mtume kufariki ile 1/5 ilikuwa inakwenda kwa Khalifa au Imam ambaye huigawanya, sehemu akachukua mwenyewe na sehemu zingine akawapa ndugu za Mtume s.a.w na mayatima, maskini na wasafiri. Si lazima mafungu yawe sawasawa, kwa rai ya Imam Malik na kwa namna ilivyokuwa ikigawanywa siku za Mtume *s.a.w.* bali ni juu ya Imam kugawanya kama aonavyo inafaa.

Siku ya Kipambanuzi, ni siku ya vita vya Badri. Allah alipoleta Malaika Zake kuwasaidia Waislamu na wakashinda na hali vivi hivi wasingeweza kushinda kwa hali ya unyonge waliokuwa nao. Siku hiyo Allah alipambanua ni kundi gani linashika haki.

Aya 44. Waislamu walipokuwa wakienda Badri, Mtume akaona katika ndoto kuwa jeshi

وَلَوْ اَرٰىكَهُمْ كَثِيْرًا لَّفَشِلْتُمْ وَلَتَنَازَعْتُمْ فِى الْاَمْرِ وَلٰكِنَّ اللّٰهَ سَلَّمَ ؕ اِنَّهٗ عَلِيْمٌۢ بِذَاتِ الصُّدُوْرِ ﴿۴۳﴾

Angalikuonyesha kwamba wao ni wengi mngalitenguka nguvu na mngalizozana katika jambo hilo. Lakini Allah Alilinda. Bila shaka Yeye ni Mjuzi wa yaliyomo vifuani.

وَاِذْ يُرِيْكُمُوْهُمْ اِذِ الْتَقَيْتُمْ فِىْٓ اَعْيُنِكُمْ قَلِيْلًا وَّيُقَلِّلُكُمْ فِىْٓ اَعْيُنِهِمْ لِيَقْضِىَ اللّٰهُ اَمْرًا كَانَ مَفْعُوْلًا ؕ وَاِلَى اللّٰهِ تُرْجَعُ الْاُمُوْرُ ﴿۴۴﴾ ع

45. Na (kumbukeni) Alipowaonyesheni machoni mwenu mlipokutana, kwamba wao ni wachache na Akawafanyeni kuwa wachache machoni mwao, ili Allah Alitimize jambo lililokuwa litendeke. Na mambo yote hurejeshwa kwa Allah.

FUNGU 6

يٰٓاَيُّهَا الَّذِيْنَ اٰمَنُوْٓا اِذَا لَقِيْتُمْ فِئَةً فَاثْبُتُوْا وَاذْكُرُوا اللّٰهَ كَثِيْرًا لَّعَلَّكُمْ تُفْلِحُوْنَ ﴿۴۵﴾ ع

46. Enyi mlioamini, mkutanapo na jeshi, basi kuweni imara, na mumkumbuke Allah kwa wingi ili mpate kufaulu.

---

la adui ni dogo kuliko la Waislamu (Jarir jalada 10, uk. 9). Katika tafsiri ya ndoto, maana ya ndoto hii ni kuwa jeshi la watu wa Makka litashindwa juu ya ukubwa wake na zana zake. Kama adui angeonyeshwa katika ndoto kuwa ni watu wengi, tafsiri ya ndoto ingekuwa hivi, upande wa aliyeota ndoto utakufa moyo na utashindwa na adui.

Aya 45. Pande hizi mbili zilipokutana ana kwa ana, Waislamu wakaona sehemu mbili tu za jeshi la maadui 1,000 ambao walikuwa wamewaficha sehemu yao nyingine ili Waislamu wasije kuwaona ni wengi mno wakaingia woga na kuwakimbia. Makafiri walitumia hila hii Waislamu wathubutu kupigana wapate kuwafuta kabisa.

Kumbe Waislamu walipowaona si wengi, wakapata moyo wa kupigana nao. Isitoshe, makafiri waliliona jeshi la Waislamu 313 kuwa dogo mno, wakalidharau. Makafiri wakadharau, Waislamu wakakazana. Pande zote mbili zikapata ujasiri wa kupambana. Jambo aliloamuru Allah litendeke, likatendeka kwa mwujiza huu, na makafiri wakashindwa.

Sura 3: 14 pia inaeleza kuwa Waislamu ndio walioonekana wachache. Basi hakuna hitilafu yo yote kama anavyoonekana kudhani Padre Dale.

Aya 46. *Mumkumbuke Allah kwa wingi*. Ndio kusema, adui ataleta wasaidizi wake na waaminio watake msaada wa Allah kwa kumwomba kila wakati. Katika mashindano mumini hatakiwi kutegemea vifaa vyake tu, bali kumwomba sana Allah na kumtegemea Yeye.

47. Na Mtiini Allah na Mtume Wake wala msigombane, waila mtakuwa waoga na haiba yenu itapotea, na vumilieni. Bila shaka Allah Yu pamoja na wavumilivu.

وَاَطِيْعُوا اللّٰهَ وَرَسُوْلَهٗ وَلَا تَنَازَعُوْا فَتَفْشَلُوْا وَتَذْهَبَ رِيْحُكُمْ وَاصْبِرُوْا ؕ اِنَّ اللّٰهَ مَعَ الصّٰبِرِيْنَ ﴿۴۶﴾

48. Wala msiwe kama wale waliotoka katika majumba yao kwa fahari na kujionyesha kwa watu na kuwazuilia watu njia ya Allah, na Allah Ameyazunguka wanayoyafanya.

وَلَا تَكُوْنُوْا كَالَّذِيْنَ خَرَجُوْا مِنْ دِيَارِهِمْ بَطَرًا وَّرِئَآءَ النَّاسِ وَيَصُدُّوْنَ عَنْ سَبِيْلِ اللّٰهِ ؕ وَاللّٰهُ بِمَا يَعْمَلُوْنَ مُحِيْطٌ ﴿۴۷﴾

49. Na (kumbukeni) Shetani alipowapambia vitendo vyao, na kusema: Leo hakuna wa kuwashindeni katika watu, na hakika mimi ni mlinzi wenu. Lakini yalipoonana majeshi mawili, (Shetani) akarudi nyuma na kusema: Mimi si pamoja nanyi, hakika mimi naona msiyoyaona, bila shaka mimi ninamwogopa Allah; na Allah ni Mkali wa kuadhibu.

وَاِذْ زَيَّنَ لَهُمُ الشَّيْطٰنُ اَعْمَالَهُمْ وَقَالَ لَا غَالِبَ لَكُمُ الْيَوْمَ مِنَ النَّاسِ وَاِنِّيْ جَارٌ لَّكُمْ ۚ فَلَمَّا تَرَآءَتِ الْفِئَتٰنِ نَكَصَ عَلٰى عَقِبَيْهِ وَقَالَ اِنِّيْ بَرِيْٓءٌ مِّنْكُمْ اِنِّيْٓ اَرٰى مَا لَا تَرَوْنَ اِنِّيْٓ اَخَافُ اللّٰهَ ؕ وَاللّٰهُ شَدِيْدُ الْعِقَابِ ﴿۴۸﴾ ع ۶

FUNGU 7

50 (Kumbukeni) waliposema wanafiki na wale wenye ugonjwa mioyoni mwao: Watu hawa dini yao imewadanganya. Na mwenye kutegemea kwa Allah, basi kwa yakini Allah ndiye Ashindaye, Mwenye hekima.

اِذْ يَقُوْلُ الْمُنٰفِقُوْنَ وَالَّذِيْنَ فِيْ قُلُوْبِهِمْ مَّرَضٌ غَرَّ هٰٓؤُلَآءِ دِيْنُهُمْ ؕ وَمَنْ يَّتَوَكَّلْ عَلَى اللّٰهِ فَاِنَّ اللّٰهَ عَزِيْزٌ حَكِيْمٌ ﴿۴۹﴾

Aya 47. Waislamu wanafundishwa njia tatu za kuwafanya washinde: (1) Kutii amri za Mungu na Mtume; (2) wasigombane, wawe katika umoja; (3) wafanye subira.

Aya 48. Msiwe kama wale, yaani jeshi la watu wa Makka lililoongozwa na Abu Jahal lililotoka kwa majivuno na fahari. Waislamu wanaonywa wasiige mwenendo wa majivuno na kutaka kuonekana na watu. Katika dini yanayotakiwa ni kumzuia adui kwa shauku na jazba kwa nia ya kuisaidia haki, siyo kwa kutaka kusifiwa na watu.

Aya 49. Shetani alipowapambia vitendo vyao. Hapa Shetani mradi wake ni mtu.

وَلَوْ تَرٰٓى اِذْ يَتَوَفَّى الَّذِيْنَ كَفَرُوا ۙ
الْمَلٰٓئِكَةُ يَضْرِبُوْنَ وُجُوْهَهُمْ
وَاَدْبَارَهُمْ ۚ وَذُوْقُوْا عَذَابَ الْحَرِيْقِ ﴿٥٠﴾

51. Na laiti ungaliona Malaika watakapowafisha wale waliokufuru wakiwapiga nyuso zao na migongo yao na (kuwaambia): Ionjeni adhabu iunguzayo.

ذٰلِكَ بِمَا قَدَّمَتْ اَيْدِيْكُمْ وَاَنَّ اللّٰهَ لَيْسَ
بِظَلَّامٍ لِّلْعَبِيْدِ ﴿٥١﴾ ۙ

52. Hayo ni kwa sababu ya yale iliyoyatanguliza mikono yenu. Na hakika Allah si mwenye kuwadhulumu hata kidogo watumishi.

كَدَاْبِ اٰلِ فِرْعَوْنَ ۙ وَالَّذِيْنَ مِنْ قَبْلِهِمْ ؕ
كَفَرُوْا بِاٰيٰتِ اللّٰهِ فَاَخَذَهُمُ اللّٰهُ بِذُنُوْبِهِمْ ؕ
اِنَّ اللّٰهَ قَوِيٌّ شَدِيْدُ الْعِقَابِ ﴿٥٢﴾

53. Ni kama hali ya watu wa Firauni na wale waliokuwa kabla yao: walizikataa Ishara za Allah, kwa hiyo Allah Akawashika kwa sababu ya madhambi yao. Bila shaka Allah ni Mwenye nguvu, Mkali wa kuadhibu.

ذٰلِكَ بِاَنَّ اللّٰهَ لَمْ يَكُ مُغَيِّرًا نِّعْمَةً
اَنْعَمَهَا عَلٰى قَوْمٍ حَتّٰى يُغَيِّرُوْا مَا
بِاَنْفُسِهِمْ ۙ وَاَنَّ اللّٰهَ سَمِيْعٌ عَلِيْمٌ ﴿٥٣﴾ ۙ

54. Hayo ni kwa sababu Allah si Mwenye kuzibadilisha neema Alizowaneemesha watu hata wabadilishe yaliyomo nafsini mwao; na ya kwamba Allah ndiye Asikiaye, Ajuaye.

كَدَاْبِ اٰلِ فِرْعَوْنَ ۙ وَالَّذِيْنَ
مِنْ قَبْلِهِمْ ؕ كَذَّبُوْا بِاٰيٰتِ رَبِّهِمْ
فَاَهْلَكْنٰهُمْ بِذُنُوْبِهِمْ وَاَغْرَقْنَآ
اٰلَ فِرْعَوْنَ ۚ وَكُلٌّ كَانُوْا ظٰلِمِيْنَ ﴿٥٤﴾

55. Ni kama hali ya watu wa Firauni na wale waliokuwa kabla yao; walizikadhibisha Ishara za Mola wao, basi Tukawaangamiza kwa sababu ya dhambi zao, na Tukawagharikisha watu wa Firauni, na wote walikuwa wadhalimu.

---

anayewapoteza wenziwe na kuwapa mashauri mabaya. Mtu huyu anayetajwa hapa ni Suraka bin Malik bin Ju'sham, mkuu wa Banu Kanana, ambaye aliwachochea watu wa Makka wapigane na Waislamu, lakini baadaye yeye mwenyewe akaingia dini ya Kiislamu.

Aya 53. Aya hii inaonyesha kuwa Allah aliwaadhibu maadui wa Uislamu katika Badri kama alivyowaadhibu maadui wa Musa. Aya hii inaonyesha namna wanavyofanana Mtume *s.a.w.* na Mtume Musa (Tazama sura 7:158).

Aya 54. Hii ndio kanuni ya Allah kwamba hawaondolei watu neema alizowapa mpaka kwanza nyoyo zao zimebadilika na wamekuwa wabaya. Kwa mfano, kama Mungu amewapa watu ufalme hawanyang'anyi mpaka wameacha wema na kuwa watu waovu.

إِنَّ شَرَّ الدَّوَآبِّ عِنْدَ اللّٰهِ الَّذِيْنَ كَفَرُوْا فَهُمْ لَا يُؤْمِنُوْنَ ﴿٥٦﴾

56. Hakika viumbe walio wabaya zaidi mbele ya Allah ni wale wanaokufuru, nao hawaamini.

اَلَّذِيْنَ عٰهَدْتَّ مِنْهُمْ ثُمَّ يَنْقُضُوْنَ عَهْدَهُمْ فِيْ كُلِّ مَرَّةٍ وَّهُمْ لَا يَتَّقُوْنَ ﴿٥٧﴾

57. Ambao umewaahidi kisha wakavunja ahadi yao kila mara, nao hawaogopi.

فَاِمَّا تَثْقَفَنَّهُمْ فِي الْحَرْبِ فَشَرِّدْ بِهِمْ مَّنْ خَلْفَهُمْ لَعَلَّهُمْ يَذَّكَّرُوْنَ ﴿٥٨﴾

58. Na ukiwadhibiti vitani, basi uwafurushe kwa hao walio nyuma yao ili wapate kukumbuka.

وَاِمَّا تَخَافَنَّ مِنْ قَوْمٍ خِيَانَةً فَانْۢبِذْ اِلَيْهِمْ عَلٰى سَوَآءٍ ؕ اِنَّ اللّٰهَ لَا يُحِبُّ الْخَآئِنِيْنَ ﴿٥٩﴾ ع

59. Na kama ukiogopa hiana kwa watu, basi uivunje (ahadi yao) kama walivyofanya; hakika Allah Hawapendi wafanyao hiana.

FUNGU 8

وَلَا يَحْسَبَنَّ الَّذِيْنَ كَفَرُوْا سَبَقُوْا ؕ اِنَّهُمْ لَا يُعْجِزُوْنَ ﴿٦٠﴾

60. Wala wale waliokufuru wasifikiri kwamba wao wameshinda; kwa yakini wao hawataweza kamwe kudhoofisha.

وَاَعِدُّوْا لَهُمْ مَّا اسْتَطَعْتُمْ مِّنْ قُوَّةٍ وَّمِنْ رِّبَاطِ الْخَيْلِ تُرْهِبُوْنَ بِهٖ عَدُوَّ اللّٰهِ وَعَدُوَّكُمْ وَاٰخَرِيْنَ مِنْ دُوْنِهِمْ ۚ لَا تَعْلَمُوْنَهُمْ ۚ اَللّٰهُ يَعْلَمُهُمْ ؕ وَمَا تُنْفِقُوْا مِنْ شَيْءٍ فِيْ سَبِيْلِ اللّٰهِ يُوَفَّ اِلَيْكُمْ وَاَنْتُمْ لَا تُظْلَمُوْنَ ﴿٦١﴾

61. Na wafanyieni maandalizi mwezavyo kwa kukusanya nguvu na kwa kufunga farasi mipakani, ambazo kwazo mnawatisha maadui wa Allah na madui zenu, na wengineo wasiokuwa wao, msiowajua, Allah Awajua. Na cho chote mtakachotoa katika njia ya Allah, mtarudishiwa sawasawa wala hamtadhulumiwa.

Aya 56. Aya hii inaieleza sura 6:39 inayosema kuwa wanyama na ndege ni bora kuliko makafiri, maana wanyama hawakupewa akili na fahamu, na makafiri wamepewa lakini hawatumii.

Aya 58. Mumini hakimbilii kupigana. Lakini anapolazimika kushika silaha anatakiwa ampige adui kwa mapigo mazito hata yeye akome, na walio nyuma yake waingie hofu.

Aya 61. Mwislamu anafundishwa kuwa kujiweka tayari kwa vita ndio njia ya kuzuia vita visitokee. Anafundishwa aweke katika nchi majeshi ya kutosha na pia majeshi yenye nguvu mipakani ili adui akiona aingie hofu, asilete wazo la kushambulia, na hivyo waaminio watakaa kwa amani.

وَاِنْ جَنَحُوْا لِلسَّلْمِ فَاجْنَحْ لَهَا وَتَوَكَّلْ عَلَى اللّٰهِ ؕ اِنَّهٗ هُوَ السَّمِيْعُ الْعَلِيْمُ ﴿٦٢﴾

62. Na kama wakielekea kwenye amani nawe pia uielekee, na Mtegemee Allah. Hakika Yeye ndiye Asikiaye, Ajuaye.

وَاِنْ يُّرِيْدُوْٓا اَنْ يَّخْدَعُوْكَ فَاِنَّ حَسْبَكَ اللّٰهُ ؕ هُوَ الَّذِيْٓ اَيَّدَكَ بِنَصْرِهٖ وَبِالْمُؤْمِنِيْنَ ﴿٦٣﴾

63. Na kama wakitaka kukuhadaa, basi Allah Atakutosheleza. Yeye ndiye Aliyekusaidia kwa nusura Yake na kwa waaminio.

وَاَلَّفَ بَيْنَ قُلُوْبِهِمْ ؕ لَوْ اَنْفَقْتَ مَا فِى الْاَرْضِ جَمِيْعًا مَّآ اَلَّفْتَ بَيْنَ قُلُوْبِهِمْ وَلٰكِنَّ اللّٰهَ اَلَّفَ بَيْنَهُمْ ؕ اِنَّهٗ عَزِيْزٌ حَكِيْمٌ ﴿٦٤﴾

64. Na Ameiunga mioyo yao; hata kama ungetoa yote yaliyomo ardhini usingeweza kuiunga mioyo yao, lakini Allah ndiye Aliyeiunga (mioyo yao). Hakika Yeye ndiye Mwenye ushindi kamili, Mwenye hekima.

يٰٓاَيُّهَا النَّبِىُّ حَسْبُكَ اللّٰهُ وَمَنِ اتَّبَعَكَ مِنَ الْمُؤْمِنِيْنَ ﴿٦٥﴾ ع

65. Ewe Nabii! Allah Anakutosha wewe na pia yule aliyekufuata katika waaminio.

FUNGU 9

يٰٓاَيُّهَا النَّبِىُّ حَرِّضِ الْمُؤْمِنِيْنَ عَلَى الْقِتَالِ ؕ اِنْ يَّكُنْ مِّنْكُمْ عِشْرُوْنَ صٰبِرُوْنَ يَغْلِبُوْا مِائَتَيْنِ ۚ وَاِنْ يَّكُنْ مِّنْكُمْ مِّائَةٌ يَّغْلِبُوْٓا اَلْفًا مِّنَ الَّذِيْنَ كَفَرُوْا بِاَنَّهُمْ قَوْمٌ لَّا يَفْقَهُوْنَ ﴿٦٦﴾

66. Ewe Nabii! wahimize waaminio juu ya kupigana vita; kama wakiwa miongoni mwenu ishirini wenye subira; watawashinda mia mbili; na kama wakiwa mia moja miongoni mwenu watawashinda elfu moja ya wale waliokufuru, maana hao ni watu wasiofahamu.

اَلْـٰٔنَ خَفَّفَ اللّٰهُ عَنْكُمْ وَعَلِمَ اَنَّ فِيْكُمْ ضَعْفًا ؕ فَاِنْ يَّكُنْ مِّنْكُمْ مِّائَةٌ صَابِرَةٌ يَّغْلِبُوْا مِائَتَيْنِ ۚ وَاِنْ يَّكُنْ مِّنْكُمْ اَلْفٌ

67. Sasa Allah Amewahafifishieni, maana Anajua ya kwamba kuna udhaifu kati yenu. Kwa hiyo wakiwa mia moja miongoni mwenu wenye subira watawash - inda mia mbili; na

Aya 62. Hapa Waislamu wanaambiwa, kama adui atataka mapatano ya amani, basi wakubali mara moja, haidhuru hata kama nia ya adui ni kutaka kuwadanganya ili kujipatia wakati wa kujiandaa zaidi. Aya hii inaonyesha ya kuwa makusudi ya Waislamu kupigana ni kutaka kujikinga tu, si kueneza dini.

Aya 67. Aya hii haivunji ile iliyotangulia bali kwa kitambo tu inawapunguzia Waislamu,

يَّغْلِبُوْٓا اَلْفَيْنِ بِاِذْنِ اللّٰهِ ؕ وَاللّٰهُ مَعَ الصّٰبِرِيْنَ ﴿٦٦﴾

wakiwa elfu moja miongoni mwenu watawashinda elfu mbili kwa idhini ya Allah. Na Allah Yu pamoja na wenye subira.

مَا كَانَ لِنَبِيٍّ اَنْ يَّكُوْنَ لَهٗٓ اَسْرٰى حَتّٰى يُثْخِنَ فِى الْاَرْضِ ؕ تُرِيْدُوْنَ عَرَضَ الدُّنْيَا ۖ وَاللّٰهُ يُرِيْدُ الْاٰخِرَةَ ؕ وَاللّٰهُ عَزِيْزٌ حَكِيْمٌ ﴿٦٧﴾

68. Haimpasi Nabii kuwa na wafungwa wa vita mpaka apigane vita ya umwagaji damu ardhini. Mnataka vitu vya dunia, hali Allah Anataka Akhera. Na Allah ni Mwenye nguvu, Mwenye hekima.

لَوْلَا كِتٰبٌ مِّنَ اللّٰهِ سَبَقَ لَمَسَّكُمْ فِيْمَآ اَخَذْتُمْ عَذَابٌ عَظِيْمٌ ﴿٦٨﴾

69. Isingalikuwa hukumu iliyotangulia kutoka kwa Allah, bila shaka ingaliwapateni adhabu kubwa kwa yale mliyoyashika.

فَكُلُوْا مِمَّا غَنِمْتُمْ حَلٰلًا طَيِّبًا ۖ وَّاتَّقُوا اللّٰهَ ؕ اِنَّ اللّٰهَ غَفُوْرٌ رَّحِيْمٌ ﴿٦٩﴾ ع

70. Basi kuleni katika vile mlivyoteka (vitani) vilivyo halali na vizuri, na Mcheni Allah; hakika Allah ni Msamehevu, Mrehemevu.

FUNGU 10

يٰٓاَيُّهَا النَّبِىُّ قُلْ لِّمَنْ فِىْٓ اَيْدِيْكُمْ مِّنَ الْاَسْرٰٓى ۙ اِنْ يَّعْلَمِ اللّٰهُ فِىْ قُلُوْبِكُمْ خَيْرًا يُّؤْتِكُمْ خَيْرًا مِّمَّآ اُخِذَ مِنْكُمْ وَيَغْفِرْ لَكُمْ ؕ وَاللّٰهُ غَفُوْرٌ رَّحِيْمٌ ﴿٧٠﴾

71. Ewe Nabii! waambie wale mateka waliomo mikononi mwenu: Kama Allah Akijua wema wo wote mioyoni mwenu, Atawapeni vizuri kuliko vilivyochukuliwa kwenu na Atawasameheni. Na Allah ni Msamehevu, Mrehemevu.

وَاِنْ يُّرِيْدُوْا خِيَانَتَكَ فَقَدْ خَانُوا اللّٰهَ مِنْ قَبْلُ فَاَمْكَنَ مِنْهُمْ ؕ وَاللّٰهُ عَلِيْمٌ حَكِيْمٌ ﴿٧١﴾

72. Na kama wanataka kukufanyia hiyana, basi walikwisha mfanyia Allah hiyana kabla, lakini Akakupa ushindi juu yao. Na Allah ni Mjuzi, Mwenye Hekima.

---

kwa sababu imani yao, ingawa ni ya kweli, nao ni waaminifu, bali si kama pale mwanzo walipokuwa wakiona miujiza ya mfululizo na kukongamana pamoja.

Aya 68. Ilikuwapo kabla ya Uislamu katika Waarabu desturi ambayo mpaka sasa inaendelea katika sehemu fulani fulani za dunia, kuwakamata watu kuwa wafungwa hata kama hakuna mapigano. Aya hii inakataza kabisa desturi hii mbovu. Lakini haikatazi kushika mateka vitani, wala haikatazi mateka kujikomboa (Tazama sura 47:5).

73. Hakika wale walioamini na wakahama, na wakajitahidi kwa mali zao na nafsi zao katika njia ya Allah; na wale waliotoa hifadhi na kusaidia, hao ndio marafiki wao kwa wao. Na wale walioamini lakini hawakuhama, ninyi hamnayo haki ya kuwa na urafiki nao mpaka wahame. Na kama wao wakiomba msaada kwenu katika dini, basi ni juu yenu kuwasaidia, isipokuwa juu ya watu ambao yapo mapatano baina yenu na wao. Na Allah Anayaona mnayoyatenda.

إِنَّ الَّذِيْنَ اٰمَنُوْا وَهَاجَرُوْا وَجٰهَدُوْا
بِاَمْوَالِهِمْ وَاَنْفُسِهِمْ فِيْ سَبِيْلِ اللّٰهِ
وَالَّذِيْنَ اٰوَوْا وَّنَصَرُوْٓا اُولٰٓئِكَ بَعْضُهُمْ
اَوْلِيَآءُ بَعْضٍ ؕ وَالَّذِيْنَ اٰمَنُوْا وَلَمْ
يُهَاجِرُوْا مَا لَكُمْ مِّنْ وَّلَايَتِهِمْ مِّنْ شَيْءٍ
حَتّٰى يُهَاجِرُوْا ۚ وَاِنِ اسْتَنْصَرُوْكُمْ فِي
الدِّيْنِ فَعَلَيْكُمُ النَّصْرُ اِلَّا عَلٰى قَوْمٍ
بَيْنَكُمْ وَبَيْنَهُمْ مِّيْثَاقٌ ؕ وَاللّٰهُ بِمَا
تَعْمَلُوْنَ بَصِيْرٌ ﴿٧٢﴾

74. Na wale waliokufuru ni marafiki wao kwa wao; msipotenda hivi itakuwapo fitina katika ardhi na machafuko makubwa.

وَالَّذِيْنَ كَفَرُوْا بَعْضُهُمْ اَوْلِيَآءُ بَعْضٍ ؕ
اِلَّا تَفْعَلُوْهُ تَكُنْ فِتْنَةٌ فِي الْاَرْضِ
وَفَسَادٌ كَبِيْرٌ ﴿٧٣﴾

75. Na wale walioamini na kuhama, na kujitahidi katika njia ya Allah, na wale waliotoa hifadhi na kusaidia, hao ndio waaminio wa haki, watakuwa na msamaha na riziki iliyo bora.

وَالَّذِيْنَ اٰمَنُوْا وَهَاجَرُوْا وَجٰهَدُوْا فِيْ
سَبِيْلِ اللّٰهِ وَالَّذِيْنَ اٰوَوْا وَّ نَصَرُوْٓا
اُولٰٓئِكَ هُمُ الْمُؤْمِنُوْنَ حَقًّا ؕ لَهُمْ
مَّغْفِرَةٌ وَّرِزْقٌ كَرِيْمٌ ﴿٧٤﴾

76. Na walioamini baadaye na wakahama na wakajitahidi pamoja nanyi, basi hao ni miongoni mwenu. Na ndugu wa damu wana haki zaidi wao kwa wao katika Kitabu cha Allah. Hakika Allah ni Mjuzi wa kila kitu.

وَالَّذِيْنَ اٰمَنُوْا مِنْۢ بَعْدُ وَهَاجَرُوْا
وَجٰهَدُوْا مَعَكُمْ فَاُولٰٓئِكَ مِنْكُمْ ؕ
وَاُولُوا الْاَرْحَامِ بَعْضُهُمْ اَوْلٰى بِبَعْضٍ فِيْ
كِتٰبِ اللّٰهِ ؕ اِنَّ اللّٰهَ بِكُلِّ شَيْءٍ عَلِيْمٌ ﴿٧٥﴾ ع ۝

Aya 74. *Msipotenda hivi,* yaani msipowasaidia Waislamu wanaodhulumiwa, na kutimiza sharti za mikataba mnayoandikiana na wasiokuwa Waislamu. Aya inaonyesha ya kuwa kama Waislamu hawatafuata fundisho hilo, basi kutatokea taabu na fujo katika nchi.

Aya 76. Aya hii inatoa fundisho jingine. Kwa kuwa Waislamu waliambiwa wao ni ndugu (sura 8:73), watu wengine wangefikiri labda wanaweza kurithiana. Basi hapa Aya inaeleza ya kuwa ndugu wa damu tu ndio wenye haki ya kurithiana.

سُوْرَةُ التَّوْبَةِ مَدَنِيَّةٌ وَّ هِيَ مِائَةٌ وَّ تِسْعٌ وَّ عِشْرُوْنَ اٰيَةً وَّ سِتَّةَ عَشَرَ رُكُوْعًا

9. SURA AT-TAUBA

Imeteremshwa Madina

Ina mafungu 16 na Aya 129

بَرَآءَةٌ مِّنَ اللّٰهِ وَرَسُوْلِهٖۤ اِلَى الَّذِيْنَ عٰهَدْتُّمْ مِّنَ الْمُشْرِكِيْنَ ۝١

1. (Hili ni) tangazo la kujitoa katika dhima, litokalo kwa Allah na Mtume Wake, kwa wale mlioahidiana nao miongoni mwa washirikina.

فَسِيْحُوْا فِى الْاَرْضِ اَرْبَعَةَ اَشْهُرٍ وَّاعْلَمُوْۤا اَنَّكُمْ غَيْرُ مُعْجِزِى اللّٰهِ ۙ وَاَنَّ اللّٰهَ مُخْزِى الْكٰفِرِيْنَ ۝٢

2. Basi tembeeni katika ardhi miezi minne, na jueni kwamba ninyi hamwezi kumdhoofisha Allah, na ya kwamba Allah ndiye Mfedheheshaji wa makafiri.

وَاَذَانٌ مِّنَ اللّٰهِ وَرَسُوْلِهٖۤ اِلَى النَّاسِ يَوْمَ الْحَجِّ الْاَكْبَرِ اَنَّ اللّٰهَ بَرِىْٓءٌ مِّنَ الْمُشْرِكِيْنَ ۙ وَرَسُوْلُهٗ ؕ فَاِنْ تُبْتُمْ فَهُوَ خَيْرٌ لَّكُمْ ۚ وَاِنْ تَوَلَّيْتُمْ فَاعْلَمُوْۤا اَنَّكُمْ غَيْرُ مُعْجِزِى اللّٰهِ ؕ وَبَشِّرِ الَّذِيْنَ كَفَرُوْا بِعَذَابٍ اَلِيْمٍ ۙ ۝٣

3. Na ni tangazo litokalo kwa Allah na Mtume Wake, kwa watu siku ya Haji kubwa ya kwamba Allah na mtume wake wako mbali na washirikina. Basi kama mkitubu ndio heri kwenu; na kama mkikengeuka, basi jueni kwamba ninyi hamwezi kumdhoofisha Allah. Na wapashe waliokufuru habari ya adhabu iumizayo.

Aya 1. *Baraa-at*, Neno hili hapa lina maana ya tangazo la kutoa uhuru au kutolewa katika kosa, au lawama au madaraka n.k.w. (Taj na Akrab). Aya hii wanaambiwa waabudu masanamu wote wa Bara Arabu pamoja na *Dhimmi* (yaani wasioamini waliokuwa wakilindwa na Waislamu ambao Waislamu waliandikiana nao mikataba). Aya inatangaza ya kuwa Mungu na Mtume Wake sasa wamejitoa katika lawama kwa maana ahadi zote zilizofungwa na Allah na Mtume Wake zimetimizwa sawasawa.

Aya 3. Tangazo lililomo katika Aya hii na Aya ifuatayo ni tofauti na lile lililomo katika Aya ya 1 na 2 ya sura hii hapo juu. Aya 1 na 2 inaeleza kujitoa katika mapatano na washirikina, na Aya hizi zinatangaza sasa hakuna ujamaa, na Mungu na Mtume wako mbali na washirikina.

Inasimuliwa ya kwamba katika mwaka wa tisa wa Hijra Mtume *s.a.w* aliporudi kutoka Tabuk alimtuma Seyidna Abubakar, Makka, kutangaza wakati wa Haji kubwa ya kuwa sasa hakuna mtu atakayeruhusiwa kuzunguka Kaaba uchi. Punde baada ya hapo sehemu ya kwanza ya sura hii iliteremshwa. Basi Mtume *s.a.w* akamtuma Seyidna Ali, Makka. Seyidna Ali baada ya kusoma Aya za kwanza za sura hii akawatangazia mahaji waliokusanyika Makka kutoka pande zote za Bara Arabu habari hizi mbili:-

4. Isipokuwa wale mlioahidiana nao miongoni mwa washirikina kisha hawakuwapunguzieni cho chote, wala hawakuwasaidia wo wote juu yenu, basi watimizieni ahadi yao mpaka muda wao; hakika Allah Huwapenda wamchao.

إِلَّا الَّذِينَ عَٰهَدتُّم مِّنَ الْمُشْرِكِينَ ثُمَّ لَمْ يَنقُصُوكُمْ شَيْـًٔا وَلَمْ يُظَٰهِرُوا عَلَيْكُمْ أَحَدًا فَأَتِمُّوٓا إِلَيْهِمْ عَهْدَهُمْ إِلَىٰ مُدَّتِهِمْ ۚ إِنَّ اللَّهَ يُحِبُّ الْمُتَّقِينَ ۝٤

5. Na miezi mitakatifu itakapopita, basi waueni washirikina po pote mwakutapo, na wakamateni na wahusuruni na waoteeni katika kila maoteo. Lakini wakitubu na kusimamisha Sala na kutoa Zaka, basi iacheni njia yao. Hakika Allah ni Msamehevu, Mrehemevu.

فَإِذَا انسَلَخَ الْأَشْهُرُ الْحُرُمُ فَاقْتُلُوا الْمُشْرِكِينَ حَيْثُ وَجَدتُّمُوهُمْ وَخُذُوهُمْ وَاحْصُرُوهُمْ وَاقْعُدُوا لَهُمْ كُلَّ مَرْصَدٍ ۚ فَإِن تَابُوا وَأَقَامُوا الصَّلَوٰةَ وَءَاتَوُا الزَّكَوٰةَ فَخَلُّوا سَبِيلَهُمْ ۚ إِنَّ اللَّهَ غَفُورٌ رَّحِيمٌ ۝٥

---

1. Anayeabudu sanamu hana ruhusa kufika katika Nyumba ya Mungu baada ya mwaka huu.
2. Mkataba na mapatano yaliyoko baina ya Mtume na wanaoabudu masanamu yataendelea kufuatwa kwa uaminifu mpaka muda wao kwisha.

Aya 4. Aya hii inawapambanua washirikina wale walioingia katika mkataba na Waislamu. Hao walikuwa makabila ya Banuu Khuzaa', Banu Mudlij, Banu Bakr, Banu Dhumra na baadhi ya Banu Sulaim.

Aya 5. *Miezi iliyokatazwa*. Kwa desturi miezi minne, *Shawwaal, Dhul-Qa'ada, Dhul-Hijja* na *Rajab,* - mitatu ya kwanza ni ya Haji kubwa, na wa mwisho ni wa Haji ndogo iitwayo Umra, - inadhaniwa kuwa ndio miezi inayokusudiwa na Aya hii (tazama sura 2:195, 218). Lakini miezi iliyosemwa hapa kuwa ilikatazwa si hiyo minne mitukufu, bali ni miezi iliyotajwa katika Aya 2 hapa juu; kwani katika siku za Mtume *s.a.w* ilimchukua mtu miezi minne kuitembelea Bara Arabu yote kwa mapana na mrefu. Hivyo katika Aya hiyo ya pili makafiri walipewa muda wa miezi minne kuizunguka Bara Arabu yote ili wajionee wenyewe mafanikio yaliyobashiriwa na Uislamu yametimia namna gani.

Wauweni washirikina po pote mwakutapo. Yaani utakapokwisha muda huo wa miezi minne, vita ianzishwe tena na wale washirikina waliovunja mapatano na kufanya hiyana, ambao walikwishakuwa katika hali ya mapigano na Waislamu, wakamatwe na kuuawa po pote wakutwapo. Ikumbukwe ya kwamba shambulio hili linaloelezwa na Aya hii halikuelekezwa kwa washirikina wote, bali wale wale waliokwisha leta vita kwa Waislamu na kuvunja mapatano na kufanya hila ya kumfukuza Mtume Madina. Sababu za kukata shauri namna hii zimeelezwa katika Aya 8 mpaka 13. Washirikina ambao hawakuvunja mapatano na kufanya hiyana walilindwa (tazama Aya 4 na 7). Juu ya hayo inasikitisha sana kuona ya kwamba baadhi ya wapinzani wa Uislamu wanaiondoa amri hii katika mpango wake na Aya nyingine, ili wapate kudanganya watu kuwa Uislamu unafundisha kuwaua watu wote wasio Waislamu.

Waoteeni katika kila maoteo. Maana ya maneno haya ni kuwa maadui wachunguliwe barabara kila wanakopita-pita, ili wasiweze kuzusha machafuko na kueneza propaganda ya ukorofi juu ya Usilamu

6. Na kama mmoja wa washirikina akikuomba ulinzi, basi mlinde mpaka asikie maneno ya Allah, kisha mfikishe mahali pake pa amani. Hayo ni kwa sababu ya kuwa hao ni watu wasiojua.

وَاِنْ اَحَدٌ مِّنَ الْمُشْرِكِيْنَ اسْتَجَارَكَ
فَاَجِرْهُ حَتّٰى يَسْمَعَ كَلٰمَ اللّٰهِ ثُمَّ اَبْلِغْهُ
مَاْمَنَهٗ ؕ ذٰلِكَ بِاَنَّهُمْ قَوْمٌ لَّا يَعْلَمُوْنَ ۝٦ ع

FUNGU 2

7. Itakuwaje ahadi kwa washirikina mbele ya Allah na mbele ya Mtume Wake isipokuwa wale mlioahidiana nao mbele ya Msikiti Mtukufu? Basi maadamu wanawanyookeeni, nanyi pia wanyookeeni; hakika Allah Huwapenda wamwogopao.

كَيْفَ يَكُوْنُ لِلْمُشْرِكِيْنَ عَهْدٌ عِنْدَ
اللّٰهِ وَعِنْدَ رَسُوْلِهٖۤ اِلَّا الَّذِيْنَ عٰهَدْتُّمْ
عِنْدَ الْمَسْجِدِ الْحَرَامِ ۚ فَمَا اسْتَقَامُوْا لَكُمْ
فَاسْتَقِيْمُوْا لَهُمْ ؕ اِنَّ اللّٰهَ يُحِبُّ الْمُتَّقِيْنَ ۝٧

8 Vipi? Hali wakiwashindeni hawataangalia kwenu udugu wala ahadi. Wanawafurahisheni kwa vinywa vyao hali mioyo yao inakataa. Na wengi wao ni waasi.

كَيْفَ وَاِنْ يَّظْهَرُوْا عَلَيْكُمْ لَا يَرْقُبُوْا
فِيْكُمْ اِلًّا وَّلَا ذِمَّةً ؕ يُرْضُوْنَكُمْ
بِاَفْوَاهِهِمْ وَتَاْبٰى قُلُوْبُهُمْ ۚ
وَاَكْثَرُهُمْ فٰسِقُوْنَ ۝٨

9. Wameziuza Ishara za Allah kwa thamani ndogo na wanaizuilia njia Yake. Hakika ni mabaya waliyokuwa wakiyafanya.

اِشْتَرَوْا بِاٰيٰتِ اللّٰهِ ثَمَنًا قَلِيْلًا فَصَدُّوْا عَنْ
سَبِيْلِهٖ ؕ اِنَّهُمْ سَآءَ مَا كَانُوْا يَعْمَلُوْنَ ۝٩

10. Hawaangalii kwa mwaminio udugu wala ahadi; na hao ndio warukao mipaka.

لَا يَرْقُبُوْنَ فِيْ مُؤْمِنٍ اِلًّا وَّلَا ذِمَّةً ؕ
وَاُولٰٓئِكَ هُمُ الْمُعْتَدُوْنَ ۝١٠

Maneno ya Aya yenyewe yanaonyesha kuwa siku zile zilikuwa za taabu sana kwa Waislamu, na upande mwingine kukawa na maadui wanaozunguka-zunguka kati ya Waislamu, wakichochea fitina na kuwachokozea mapigano - yaani washirikina. Hivyo ilikuwa lazima waangaliwe sana na kuadhibiwa sawasawa ili kuwakomesha.

Lakini wakitubu na kusimamisha Sala na kutoa Zaka. Maneno haya yanaonyesha kuwa hata wale maadui waliowatia Waislamu taabu kubwa, wakitubu na kushika Uislamu kwa hiari yao, watasamehewa. Siyo kwamba wanashurutishwa, kama inavyoonekana wazi katika Aya hiyo.

Aya 6. Aya hii inaonyesha ya kuwa Waislamu hawakupigana vita ili kuwashurutisha washirikina kuingia Uislamu. Hata katika hali ya vita, washirikina waliruhusiwa kufika Madina na kupeleleza habari za Uislamu, na kama hawakutaka kuingia walirudi makwao salama kabisa. Mbele ya ushahidi wa mafundisho yaliyo wazi kabisa kama haya, ni udhalimu mkubwa ulioje kuisingizia Islam kuwa yatia watu katika dini kwa karaha!

فَاِنْ تَابُوْا وَاَقَامُوا الصَّلٰوةَ وَاٰتَوُا الزَّكٰوةَ
فَاِخْوَانُكُمْ فِي الدِّيْنِ ؕ وَنُفَصِّلُ الْاٰيٰتِ
لِقَوْمٍ يَّعْلَمُوْنَ ﴿١١﴾

11. Na kama wakitubu na kusimamisha Sala na kutoa Zaka, basi ni ndugu zenu katika dini. Na Tunazieleza Aya kwa watu wanaojua.

وَاِنْ نَّكَثُوْٓا اَيْمَانَهُمْ مِّنْۢ بَعْدِ عَهْدِهِمْ
وَطَعَنُوْا فِيْ دِيْنِكُمْ فَقَاتِلُوْٓا اَئِمَّةَ
الْكُفْرِ ۙ اِنَّهُمْ لَآ اَيْمَانَ لَهُمْ لَعَلَّهُمْ
يَنْتَهُوْنَ ﴿١٢﴾

12. Na kama wakivunja viapo vyao baada ya kuahidi kwao na kufanya upinzani juu ya dini yenu, basi waueni viongozi wa ukafiri, hakika viapo vyao havina maana, ili wapate kujizuia.

اَلَا تُقَاتِلُوْنَ قَوْمًا نَّكَثُوْٓا اَيْمَانَهُمْ
وَهَمُّوْا بِاِخْرَاجِ الرَّسُوْلِ وَهُمْ
بَدَءُوْكُمْ اَوَّلَ مَرَّةٍ ؕ اَتَخْشَوْنَهُمْ ۚ
فَاللّٰهُ اَحَقُّ اَنْ تَخْشَوْهُ اِنْ كُنْتُمْ مُّؤْمِنِيْنَ ﴿١٣﴾
قَاتِلُوْهُمْ يُعَذِّبْهُمُ اللّٰهُ بِاَيْدِيْكُمْ
وَيُخْزِهِمْ وَيَنْصُرْكُمْ عَلَيْهِمْ وَيَشْفِ
صُدُوْرَ قَوْمٍ مُّؤْمِنِيْنَ ﴿١٤﴾
وَيُذْهِبْ غَيْظَ قُلُوْبِهِمْ ؕ وَيَتُوْبُ اللّٰهُ
عَلٰى مَنْ يَّشَآءُ ؕ وَاللّٰهُ عَلِيْمٌ حَكِيْمٌ ﴿١٥﴾

13. Je! hamtapigana na watu waliovunja viapo vyao na kufunga nia ya kumfukuza Mtume, nao ndio waliowaanzeni mara ya kwanza? Je, mnawaogopa? Basi Allah Anastahili zaidi mumuogope, ikiwa ninyi ni waaminio.

14. Piganeni nao Allah Awaadhibu kwa mikono yenu, na kuwafedhehesha, na kuwa saidieni juu yao, na Aviponye vifua vya watu waaminio;

15. Na aondoe ghadhabu ya mioyo yao; na Allah Humwelekea kwa rehema Amtakaye; na Allah ni Mjuzi, Mwenye hekima.

اَمْ حَسِبْتُمْ اَنْ تُتْرَكُوْا وَلَمَّا يَعْلَمِ اللّٰهُ
الَّذِيْنَ جٰهَدُوْا مِنْكُمْ وَلَمْ يَتَّخِذُوْا مِنْ
دُوْنِ اللّٰهِ وَلَا رَسُوْلِهٖ وَلَا الْمُؤْمِنِيْنَ
وَلِيْجَةً ؕ وَاللّٰهُ خَبِيْرٌۢ بِمَا تَعْمَلُوْنَ ﴿١٦﴾ ع

16. Je! mnadhani kuwa mtaachwa na hali Allah Hajajulisha wale waliojitahidi miongoni mwenu wala hawakumfanya rafiki wa moyo isipokuwa Allah na Mtume wake na waaminio? Na Allah Anazo habari za mnayoyafanya.

Aya 12. Kufanya upinzani juu ya dini yenu, sio mradi wake kufanya upinzani wa mdomo, bali kuleta vita na kuharibu haki kubwa za Uislamu. Neno *ta'ana* lililotumika hapa maana yake ni *kuchoma kwa mkuki.*

Aya 13. *Kumfukuza Mtume.* Waliofunga nia ya kumfukuza Mtume si Makureshi ambao kwa yakini walimfukuza hasa, bali ni wale ambao Mtume alipokwenda vitani huko mipaka ya Sham¸ wakatengeneza shauri ya kumfukuza¸ kwa kukusanya pamoja makabila yote ya Makka yasimame pamoja kumpinga atakaporudi.

FUNGU 3

مَا كَانَ لِلْمُشْرِكِيْنَ اَنْ يَّعْمُرُوْا مَسٰجِدَ
اللّٰهِ شٰهِدِيْنَ عَلٰٓى اَنْفُسِهِمْ بِالْكُفْرِ ؕ
اُولٰٓئِكَ حَبِطَتْ اَعْمَالُهُمْ ۚ وَ فِى النَّارِ
هُمْ خٰلِدُوْنَ ﴿١٧﴾

17. Washirikina hawawezi kuistawisha misikiti ya Allah hali wanajishuhudia ukafiri. Hao ndio vitendo vyao vimeharibika na katika Moto wao watakaa.

اِنَّمَا يَعْمُرُ مَسٰجِدَ اللّٰهِ مَنْ اٰمَنَ بِاللّٰهِ
وَالْيَوْمِ الْاٰخِرِ وَ اَقَامَ الصَّلٰوةَ وَاٰتَى
الزَّكٰوةَ وَلَمْ يَخْشَ اِلَّا اللّٰهَ ۖ فَعَسٰٓى
اُولٰٓئِكَ اَنْ يَّكُوْنُوْا مِنَ الْمُهْتَدِيْنَ ﴿١٨﴾

18. Anayestawisha misikiti ya Allah ni yeye tu amuaminiye Allah na Siku ya mwisho, na kusimamisha Sala na kutoa Zaka na hamuogopi ye yote ila Allah; basi hao huenda wakawa miongoni mwa walioongozwa.

اَجَعَلْتُمْ سِقَايَةَ الْحَآجِّ وَعِمَارَةَ الْمَسْجِدِ
الْحَرَامِ كَمَنْ اٰمَنَ بِاللّٰهِ وَالْيَوْمِ الْاٰخِرِ
وَجٰهَدَ فِىْ سَبِيْلِ اللّٰهِ ؕ لَا يَسْتَوٗنَ عِنْدَ
اللّٰهِ ؕ وَاللّٰهُ لَا يَهْدِى الْقَوْمَ الظّٰلِمِيْنَ ﴿١٩﴾

19. Je! mnafanya kuwanywesha mahaji na kuustawisha Msikiti Mtukufu ni sawa na (kazi ya) yule anayemuamini Allah na Siku ya mwisho na akajitahidi katika njia ya Allah? Hawawi sawa mbele ya Allah. Na Allah Hawaongozi watu wadhalimu.

اَلَّذِيْنَ اٰمَنُوْا وَ هَاجَرُوْا وَ جٰهَدُوْا فِىْ
سَبِيْلِ اللّٰهِ بِاَمْوَالِهِمْ وَاَنْفُسِهِمْ ۙ اَعْظَمُ
دَرَجَةً عِنْدَ اللّٰهِ ؕ وَاُولٰٓئِكَ هُمُ الْفَآئِزُوْنَ ﴿٢٠﴾

20. Wale walioamini na wakahama na kufanya juhudi katika njia ya Allah kwa mali zao na kwa nafsi zao wana cheo kikubwa mbele ya Allah; na hao ndio watakaostawi.

يُبَشِّرُهُمْ رَبُّهُمْ بِرَحْمَةٍ مِّنْهُ وَ رِضْوَانٍ
وَّجَنّٰتٍ لَّهُمْ فِيْهَا نَعِيْمٌ مُّقِيْمٌ ﴿٢١﴾

21. Mola wao Huwapa habari njema za rehema zitokazo Kwake, na radhi, na Bustani ambazo humo watapata neema zitakazodumu.

خٰلِدِيْنَ فِيْهَآ اَبَدًا ؕ اِنَّ اللّٰهَ عِنْدَهٗٓ اَجْرٌ
عَظِيْمٌ ﴿٢٢﴾

22. Watakaa humo milele. Hakika Allah Kwake kuna malipo makubwa.

Aya 19. Kwa mafundisho ya Kiislamu, kama mtu hamwamini Allah na Mtume, lakini anafanya kazi ndogo-ndogo kama kuangalia majumba ya ibada na kutoa fedha kwa ajili ya kazi ya dini, ni jambo lisilo na faida kubwa. Kwa sababu hii Mtume *s.a.w* alisema: "Mumini ni mtakatifu zaidi kuliko Kaaba" (Ibni Majah).

يٰٓاَيُّهَا الَّذِيْنَ اٰمَنُوْا لَا تَتَّخِذُوْٓا اٰبَآءَكُمْ وَاِخْوَانَكُمْ اَوْلِيَآءَ اِنِ اسْتَحَبُّوا الْكُفْرَ عَلَى الْاِيْمَانِ ۭ وَمَنْ يَّتَوَلَّهُمْ مِّنْكُمْ فَاُولٰۗىِٕكَ هُمُ الظّٰلِمُوْنَ ۝۲۳

23. Enyi mlioamini! msiwashike baba zenu na ndugu zenu kuwa marafiki ikiwa wanapenda kufuru kuliko imani. Na miongoni mwenu atakayewafanya rafiki, basi hao ndio wadhalimu.

قُلْ اِنْ كَانَ اٰبَاۗؤُكُمْ وَاَبْنَاۗؤُكُمْ وَاِخْوَانُكُمْ وَاَزْوَاجُكُمْ وَعَشِيْرَتُكُمْ وَاَمْوَالُۨ اقْتَرَفْتُمُوْهَا وَتِجَارَةٌ تَخْشَوْنَ كَسَادَهَا وَمَسٰكِنُ تَرْضَوْنَهَآ اَحَبَّ اِلَيْكُمْ مِّنَ اللّٰهِ وَرَسُوْلِهٖ وَجِهَادٍ فِيْ سَبِيْلِهٖ فَتَرَبَّصُوْا حَتّٰى يَاْتِيَ اللّٰهُ بِاَمْرِهٖ ۭ وَاللّٰهُ لَا يَهْدِي الْقَوْمَ الْفٰسِقِيْنَ ۝۲۴ۧ

24. Sema: Kama baba zenu, na wana wenu, na ndugu zenu, na wake zenu, na jamaa zenu, na mali mlizochuma, na biashara mnazoogopa kusimama, na majumba mnayoyapenda ni vipenzi zaidi kwenu kuliko Allah na Mtume wake na kufanya juhudi katika njia Yake, basi ngojeni mpaka Allah Alete amri Yake, na Allah Hawaongozi watu waasi.

FUNGU 4

لَقَدْ نَصَرَكُمُ اللّٰهُ فِيْ مَوَاطِنَ كَثِيْرَةٍ ۙ وَّيَوْمَ حُنَيْنٍ ۙ اِذْ اَعْجَبَتْكُمْ كَثْرَتُكُمْ فَلَمْ تُغْنِ عَنْكُمْ شَيْـــًٔا وَّضَاقَتْ عَلَيْكُمُ الْاَرْضُ بِمَا رَحُبَتْ ثُمَّ وَلَّيْتُمْ مُّدْبِرِيْنَ ۝۲۵ۚ

25. Bila shaka Allah Amekwisha wasaidieni katika mapigano mengi na siku ya Hunain,ambapo uwingi wenu uliwafakharisheni, lakini haukuwafaeni cho chote, na ardhi ikawa finyu juu yenu ingawa ilikuwa yenye wasaa, kisha mkageuka mkirudi nyuma.

Aya 24. Kuwapenda ndugu na vitu vya kidunia kusimzuie mumini kuitumikia dini ya Kiislamu. Amri ya Allah inayosemwa hapa ilifika baada ya Mtume *s.a.w* kufariki, wakati watu walioingia dini kwa sababu ya faida ya dunia walipoiasi serikali na wakaadhibiwa na Allah kwa mkono wa Seyidna Abu Bakar.

Aya 25. *Hunain* ni mahali palipokuwa mapigano yenye maana sana baina ya Mtume *s.a.w* na makabila fulani ya Waarabu washirikina . Hunain ni mahali palipo kusini-mashariki maili 16 kutoka Makka.

Makka iliposhindwa na Waislamu, makabila yenye nguvu ya Hawazin na Banu Thakif walihofu isije Uislamu ukaimarika katika Hijaz. Wakaunganisha majeshi yao wakaondoka ili kwenda kuwashambulia Waislamu. Mtume *s.a.w* pamoja na watu 12,000 ambao 2,000 wao walikuwa Waislamu wapya, waliondoka na wakakutana nao mahali panapoitwa Hunain. Maadui walikuwa 20,000. Kinyume na desturi ya Mtume, watu hawa 2,000 wakaanza kuwashambulia maadui, lakini wakaelemewa upesi sana na wakakimbia kutoka uwanja wa vita wakitawanyika ovyo. Jeshi la Waislamu lililokuwa linapita katika njia nyembamba likija, lilikumbwa na watu hao 2,000, likaingia kiwewe, likatimka mbio. Mtume *s.a.w* alisimama pale pale alipokuwa, kama mwamba, pamoja na watu 100, katika kiwanja cha vita.

ثُمَّ اَنْزَلَ اللّٰهُ سَكِيْنَتَهٗ عَلٰى رَسُوْلِهٖ
وَعَلَى الْمُؤْمِنِيْنَ وَاَنْزَلَ جُنُوْدًا لَّمْ
تَرَوْهَا وَعَذَّبَ الَّذِيْنَ كَفَرُوْا ؕ وَذٰلِكَ
جَزَآءُ الْكٰفِرِيْنَ ﴿٢٦﴾

26. Kisha Allah Akateremsha utulivu Wake juu ya Mtume Wake na juu ya waaminio, na Akateremsha majeshi ambayo hamkuyaona, na Akawaadhibu wale waliokufuru, na hayo ndio malipo ya makafiri.

ثُمَّ يَتُوْبُ اللّٰهُ مِنْۢ بَعْدِ ذٰلِكَ عَلٰى مَنْ
يَّشَآءُ ؕ وَاللّٰهُ غَفُوْرٌ رَّحِيْمٌ ﴿٢٧﴾

27. Kisha baada ya haya Allah Atamwelekea Amtakaye. Na Allah ni Msamehevu, Mrehemevu.

يٰۤاَيُّهَا الَّذِيْنَ اٰمَنُوْۤا اِنَّمَا الْمُشْرِكُوْنَ
نَجَسٌ فَلَا يَقْرَبُوا الْمَسْجِدَ الْحَرَامَ بَعْدَ
عَامِهِمْ هٰذَا ۚ وَاِنْ خِفْتُمْ عَيْلَةً فَسَوْفَ
يُغْنِيْكُمُ اللّٰهُ مِنْ فَضْلِهٖۤ اِنْ شَآءَ ؕ اِنَّ اللّٰهَ
عَلِيْمٌ حَكِيْمٌ ﴿٢٨﴾

28. Enyi mlioamini! hakika washirikina ni najisi, kwa hiyo wasiukaribie Msikiti Mtukufu baada ya mwaka wao huu. Na kama mkihofia umaskini, basi hivi karibuni Allah Atawatajirisheni kwa fadhili Zake Akipenda. Hakika Allah ni Mjuzi, Mwenye hekima.

قَاتِلُوا الَّذِيْنَ لَا يُؤْمِنُوْنَ بِاللّٰهِ وَلَا بِالْيَوْمِ
الْاٰخِرِ وَلَا يُحَرِّمُوْنَ مَا حَرَّمَ اللّٰهُ
وَرَسُوْلُهٗ وَلَا يَدِيْنُوْنَ دِيْنَ الْحَقِّ مِنَ
الَّذِيْنَ اُوْتُوا الْكِتٰبَ حَتّٰى يُعْطُوا
الْجِزْيَةَ عَنْ يَّدٍ وَّهُمْ صٰغِرُوْنَ ﴿٢٩﴾ ع

29. Piganeni na wale wasiomuamini Allah wala Siku ya mwisho wala hawaharamishi Alivyoviharamisha Allah na Mtume Wake, wala hawashiki dini ya haki, miongoni mwa wale waliopewa Kitabu, mpaka watoe kodi kwa mikono yao wenyewe hali wakitii ya kwamba wameukubali utawala.

Mishale ya maadui ilimteremkia kama mvua kila upande. Huo ulikuwa wakati wa hatari sana. Lakini Mtume *s.a.w.* alimchochea nyumbu wake kuwaendea adui bila kujali, akipiga kelele kwa sauti kubwa kabisa, akisema; "Mimi ni Nabii, hakuna uwongo ndani yake, mimi ni mtoto wa Abdul Muttalib." Abbas, baba mdogo wa Mtume aliyekuwa na sauti kubwa sana, akawapigia kelele Waislamu wasimame na warudie kwa Mtume wao anayewaita. Waislamu kana kwamba wamesikia baragumu ya siku ya kufufuliwa, wakarudi haraka na wakamkazia adui vita mpaka naye hakuona njia ila kukimbia ovyo. Hapo Waislamu wakashinda vita, na maadui 6,000 wakashikwa mateka (Tabari na Hisham).

Aya 29. Aya hii inawahusu Mayahudi na Wakristo walioishi Bara Arabu. Islam ilitaka ya kwamba katika Bara Arabu, nchi iliyozaliwa Uisalmu na Makao makuu yake, kusiwe na washirikina; bali watu wa Kitabu tu ndio wawe raia. Na katika falme za Uislamu zilizoko nje ya Bara Arabu watu wote wasio Waislamu wawe raia na watozwe kodi kama desturi ya serikali zote.

FUNGU 5

30. Na Mayahudi walisema: Uzeir ni mwana wa Allah; na Wakristo walisema, Masihi ni mwana wa Allah; hayo ni maneno ya vinywa vyao tu, wanayaiga maneno ya wale waliokufuru zamani. Allah Awaangamize! Wanageuziwa wapi!

وَقَالَتِ الْيَهُوْدُ عُزَيْرُ ۨ ابْنُ اللّٰهِ وَقَالَتِ
النَّصٰرَى الْمَسِيْحُ ابْنُ اللّٰهِ ؕ ذٰلِكَ قَوْلُهُمْ
بِاَفْوَاهِهِمْ ۚ يُضَاهِـُٔوْنَ قَوْلَ الَّذِيْنَ
كَفَرُوْا مِنْ قَبْلُ ؕ قٰتَلَهُمُ اللّٰهُ ۚ اَنّٰى
يُؤْفَكُوْنَ ۝٣٠

WALITOZWA KODI KWA KUWA WALILINDWA.

Katika Aya hii Waislamu wanaamrishwa kupambana na Mayahudi na Wakristo waliokuwa Bara Arabu ambao walileta uadui juu ya Uislamu na machafuko mengi. Hivyo Waislamu waliambiwa wapigane na watu hao wanaoshika dini isiyo haki na waliokosa madaraka ili waletwe chini ya serikali yenye madaraka ya Kiislamu, na fitina na machafuko yaishe katika nchi, na kila mmoja afuate dini yake kwa amani. Na kwa kuwa ni haki ya kila raia kulipa kodi ili serikali iwe na nguvu ya kutosha kumlinda na kumnufaisha, hawa raia wa serikali ya Kiislamu ya Bara Arabu, ambao ni watu wa Kitabu, walitozwa kodi nyepesi iliyoitwa *Jizya*. Waislamu wenyewe hutoa Zaka ambayo ni kodi kubwa zaidi kuliko *jizya*, na zaidi ya hayo Waislamu tu ndio waliokuwa na lazima ya kwenda vitani kama askari wakati maadui walileta vita. Na watu wa Kitabu ambao waliitwa *Dhimmi* hawakuwa na lazima hiyo. Hivyo, kulindwa kwao na Uislamu kuliwapa raha sana, maana vita za siku hizo zilikuwa kitu cha taabu kupita kiasi. (Tazama maelezo ya sura 22:40).

Kuhakikisha ya kuwa *jizya* ilichukuliwa kwa watu wa Kitabu kwa sababu ya kuwalinda, tutataja hapa tukio moja katika habari za Waislamu wa zamani. Majeshi ya Waislamu yaliyokuwa Hims yalizidiwa nguvu na majeshi ya Warumi. Amiri wa Waislamu, Abu Ubeida, aliwaitisha wakubwa wa mji huo na akawaambia ya kuwa anasikitika hawezi kuwalinda; na kwa ajili hiyo anarudisha kodi yote iliyotolewa na watu wao, na akaitoa kuwapa (The Caliphate, Sir William Muir).

Ni wazi ya kuwa si mradi wa Aya hii kuwa Wakristo na Mayahudi wapigwe kwa sababu hawana dini ya haki; kwani safari moja Mtume aliposikia Wakristo wa dola ya Kirumi wanaleta majeshi kushambulia Waislamu, aliondoka na jeshi mpaka Tabuk. Huko akakuta ya kwamba habari alizosikia hazikuwa kweli, basi alirudi na hakuwashambulia. Hivyo, Aya hii ingekuwa na amri ya kuwapiga kwa sababu ya hitilafu ya dini wale Warumi wasingeachwa bila kushambuliwa. Kupigwa kwa Wakristo na Mayahudi ni kwa sababu walileta machafuko nchini na kuwasumbua Waislamu bure.

Aya 30. *'Uzeir ni mwana wa Mwenyezi Mungu.* 'Uzeir ndiye Ezra anayetajwa katika Biblia. Baadhi ya Mayahudi wa Madina walikuwa na itikadi ya kuwa 'Uzeir ni mwana wa Mungu. Kadhalika katika Hadhramaut kulikuwa madhehebu moja ya Mayahudi waliosadiki kuwa 'Uzeir ni mwana wa Mungu. Mayahudi hao waliendelea kuwepo kwa uchache mpaka mwisho wa karne ya nne ya Hijra (Qastalani na Dawud Zaahir). Kwa kuwa itikadi hii ya Mayahudi inayoonekana kuwa ya kikundi maalum ni kitu walichozua baadaye haikuweza kudumu zaidi na vitabu vya leo vya Mayahudi haviitaji. Mahali pengine Qur'an inasema Waisraeli walikuwa wepesi kumpa Mungu watoto. (sura 5:19).

Masihi ni mwana wa Allah. Biblia imetumia 'mwana wa Mungu' kwa watu wengi (tazama maelezo ya sura 5:19). Kwa kuwa Wakristo wamebuni itikadi ya utatu wa Mungu, hawataki kuwaita wengine wana wa Mungu, maana wakifanya hivyo wanaona miungu itakuwa mingi mno. Ni vigumu kusadiki kwamba Yesu ni mwana wa Mungu wa pekee hali wako wengine walioitwa wana wa Mungu yule yule aliyemwita Yesu mwanawe. Wakristo hawakubali kwamba Mariam aliyemzaa Yesu alikuwa mke wa Mungu, ijapokuwa Wakatoliki wamempandisha mbinguni. Basi kama ni kuitwa tu kulikompa Yesu uwana wa Mungu, basi wengine walioitwa hivyo pia wanastahili wasinyang'anywe haki ya kuitwa wana wa Mungu.

YESU ANAYO MAJINA MENGI.

Wakristo wamedanganyika na maneno ya methali yaliyotumika katika Injili. Yesu aliitwa "mlango" (Yohana 10:8); aliitwa "mkate" (Yohana 6:51); aliitwa "mzabibu" (Yohana 15:1); aliitwa "mwanga" (Yohana 8:12); mahali pengine ameitwa "mwana kondoo" (Yohana 1:36); yeye mwenyewe alijiita "mchungaji" (Yohana 10:11). Na mara nyingi alijiita "mwanadamu" (Matt. 18:11; 8:20; 11:19; 17:12; 24:27, 30, 37, 39, 44; 16:28; Marko 13:26; Luka 6:15; 7:34; 17:22, 24, 26, 30; 18:8; 19:10; Yohana 3:13, 14). Wakristo wanajaribu kueleza maana za majina hayo yote, hawachukui maneno hayo katika maana zao za asili. Mbona hawasemi ya kwamba Yesu hakuwa mwanadamu, alikuwa "mti" maana alijiita "mzabibu"? Kadhalika mtu angeweza kukataa utu wake na kuhubiri ya kuwa alikuwa "mnyama" kwa sababu aliitwa "mwana kondoo." Je, Wakristo watapenda kusikia maelezo hayo ya Injili? Kama kusema hivyo ni upotevu, basi wakumbuke kwamba kumwita mwanadamu, Mungu, ni upotevu mkubwa zaidi.

MAANA YA "MWANA WA MUNGU."

Katika Injili Yesu mwenyewe ameeleza maana ya "mwana wa Mungu." Siku moja yeye aliwaambia Mayahudi kwamba: "Mimi na baba tu mmoja." Mayahudi walitaka kumpiga mawe wakisema amekufuru. Yesu aliwaambia: "Haikuandikwa katika Torati: Mimi nimesema mu miungu ninyi? Ikiwa wale waliofundishwa na Mungu waliitwa miungu, na maandiko hayatanguki, mbona mnamwambia yule aliyetakaswa na Baba na kutumwa duniani kwamba; una kufuru kwa sababu nimesema: Ni mwana wa Mungu mimi?"(Yohana10:30-36). Hapa Yesu anasema ya kwamba yeye hakudai cheo kikubwa kuliko watu wa zamani walioitwa "miungu" (Zaburi 82:6); kwani yeye alijiita "mwana wa Mungu" tu.

Kwa hakika Injili imetumia neno "mwana wa Mungu" kwa ajili ya mtu mwema; na watu wabaya wameitwa wana wa Shetani. Mayahudi waliobishana na Yesu walisema, "Baba yetu ni mmoja: Mungu" (Yohana 8:41). Yesu aliwajibu, akasema, "Ninyi mmetoka kwa baba yenu shetani" (Yohana 8:44),kwa sababu walimkadhibisha Nabii wa Mungu. Je,Wakristo wako tayari kupokea maelezo hayo ya Yesu?

Qur'an haikuwaonea Wakristo ilipowalaumu kuwa wanamwita Yesu mwana wa Mungu kwa maana isiyofaa. Akili yote inakubaliana na maelezo ya Qur'an juu ya jambo hili. Na mapadre bila shaka wanastahili kulaumiwa kwa kuwapoteza watu hali wanajua kuwa fundisho hili haliingii akilini, na ni makosa matupu.

Wanayaiga maneno ya wale waliokufuru zamani. Hakuna shaka ya kwamba Ukristo unaoonekana leo, sio ule uliofundishwa na Yesu. Katika maelezo ya sura 3:50 utaona ya kwamba Paulo aliacha maagizo ya Yesu ya kuhubiri kwa Mayahudi peke yao, akaanza kuingia katika mataifa ya wapagani. Na Paulo mwenyewe amesema ya kuwa anapokwenda kwa mataifa, anajifanya kama mtu wa mataifa (tazama maelezo ya sura 3:50). Huyo Bwana Paulo hakuwa na msingi mzuri wa mafundisho ya Yesu kwa kuwa hakuweza kujifunza kitu kwa Yesu. Zamani zile ibada iliyoshika sana katika nchi mbalimbali ni ya kuabudu jua na sayari nyingine za angani. Hii Jumapili inayoitwa kwa Kiingereza "Sunday" (Sun Day, yaani Siku ya Jua) ilikuwa siku mashuhuri ya kumwabudu mungu-Jua miongoni mwa wapagani; na hivyo ikaitwa "Sunday" yaani, "Siku ya kuliabudu Jua." Siku hizo kulikuwa mahekalu mengi sana ya huyu mungu-Jua aliyejulikana kwa

majina mengi. Wagiriki walimwita Apollo au Dionysus; Warumi walimwita Hercules; Waajemi walimwita Mithra; katika nchi ya Syria (Sham) aliitwa Adonis; katika Frigia (Phrygia) aliitwa Attis; katika Misri aliitwa Osiris, Isis na Horus; Wababelonia (watu wa nchi ya Babil) walimwita Baal; na Wakarthago walimwita Astarte.

Dini ya Mithra ilifika nchi za Wazungu kutoka Ajemi ilikokuwa imestawi kwa miaka 600, na ikafika Rumi miaka 70 kabla ya Yesu na ikaenea katika dola yao mpaka Uingereza. Mabaki ya mahekalu ya dini ya Mithra yanapatika katika sehemu za Uingereza (Encyclopaedia of Religion and Religions by Royston Pike) kama katika mji wa York, Chester na kwingineko.

UKRISTO KATIKA NYAYO ZA UPAGANI.

Mila za dini hiyo ya kipagani ya zamani ndizo zilizochukuliwa na Ukristo, na ibada zake zimekuwa sehemu ya dini ya Kikristo mpaka leo. Kwa mfano huyo Mithra alisadikiwa kuwa "Mwamuzi mkubwa baina ya Mungu na watu." Alizaliwa katika pango tarehe 25 Desemba. Alizaliwa na Bikira. Alisafiri sana. Alikuwa na wanafunzi kumi na mbili. Alikufa katika kuwatumikia watu. Alizikwa lakini akafufuka toka kaburini. Kufufuka kwake kulisherehekewa sana" (Robertson. Pagan Christs, uk. 338).

Edward Carpenter anasema ya kuwa karibu miungu wote hao wa kipagani walisadikiwa kuwa : (1) Walizaliwa siku ya Krismas au karibu sana nayo. (2) Walishuka Jahanamu. (3) Walifufuka toka wafu na kupaa mbinguni. (4) Waliweka Kommunio za Watakatifu na Makanisa yaliyopokea wanafunzi kwa kuwabatiza. (5) Walikumbukwa kwa chakula na Ekarist (Eucharist).

Mila hizi za washenzi wa zamani zimechukuliwa na kufanywa za Wakristo, hasa na Wakatoliki. Angalia kupatana kwa mafundisho ya wapagani wa zamani na ya Wakristo!

Mithra aliitwa *Mwokozi na Mwana kondoo.* Watu waliingizwa dini yake kwa kubatizwa na karamu za Sakramenti zilifanywa kwa ukumbusho wake.

DINI HIYO ILIENEA SANA ZAMANI.

Mkristo wa leo anaweza kushuku habari hizi kwa kuwa haoni alama za hiyo dini ya Mithra iliyokuwa imekwisha tangaa kabla ya Ukristo kupata nguvu. Lakini dini hiyo ilikuwa na nguvu sana katika karne ya tatu baada ya Yesu; na kama isingalizuiwa na wakristo kwa nguvu ya silaha katika Rumi na Alexandria, hata vitabu vya dini hiyo vingi vikachomwa katika Alexandria, na mwalimu mkubwa wa dini hiyo ya Jua aliyeitwa Hypatia akauawa, leo hii ukristo usingekuwa na nafasi ya kutumia mafundisho na desturi za dini ya Jua kwa jina la Ukristo; wala usingepata nafasi ya kustawi. Hata hivyo, Ukristo ulikubalika kwa watu baada ya kuwa umekwisha jaa tele mafundisho ya kipagani ambayo watu waliyapenda, uliyoyachukua na kuyafanya ya Kikristo (Robertson , Pagan Christs, uk. 350).

USHUHUDA WA TERTULLIAN.

Kupatana kwa dini ya Kikristo na dini ile ya kishenzi kunakubaliwa na mapadre pia, ingawa wao wanaona shetani ndiye wa kulaumiwa katika kupatana huko. Kwa mfano Tertullian amesema, "Shetani, ambaye kazi yake ni kuzuia haki, anaiga barabara Sakrimenti za Kiungu kuzitia katika siri za miungu ya masanamu. Naye anawabatiza, yaani wamwaminio na wamfuatao, anaahidi kusamehe dhambi toka maji matakatifu, na kuwaingiza katika dini ya Mithra. Hivyo anatia alama vipaji vya askari zake mwenyewe, anaadhimisha sadaka ya mkate; anaingiza mfano wa kufufuka, na anapata taji kwa upanga. Kasisi wake mkubwa amemzuilia mke mmoja, hata anao mabikira wake watawa" (Our Sun-God p. 179).

WAKRISTO WAKUBWA NA MAPADRE WANASHUHUDIA.

Justin Shahidi alipomwandikia Mfalme Adrian alileta udhuru kama huo wa kumtupia lawama Shetani kuwa ndiye aliyefanya hila ya kuupatanisha Ukristo na upagani. Anasema: "Ilipofikia

masikio ya Shetani kuwa manabiiwalitabiri kufika kwa Kristo (Mwana wa Mungu), akawaweka watunga mashairi wa ushenzini wawalete wengi sana watakaoitwa wana wa Jove (Jove ni mungu wa Kirumi). Shetani akafanya mpango huu ili kuwafanya watu wafikiri ya kwamba historia ya kweli ya Kristo ni ya namna moja na hadithi nyingi za ajabu za wana wa Jove. . . . Kwa kusema Neno, mzaliwa wa kwanza wa Mungu, Bwana wetu Yesu, kuzaliwa na bikira pasipo mchanganyiko wo wote wa kibinadamu, sisi (Wakristo) hatuna tusemalo zaidi katika jambo hili kuliko ninyi (wapagani) msemavyo juu ya hao mnaowaita wana wa Jove. Maana hamna haja ya kuambiwa ni wana kadiri gani ambao waandishi waliotapakaa miongoni mwenu wanawasema ni wana wa Jove. . . . Ama kwa Mwana wa Mungu anayeitwa Yesu, kama tusimruhusu kuwa zaidi kuliko mwanadamu, juu ya hayo cheo cha mwana wa Mungu ni cha haki sana, kwa sababu ya hekima yake, tukipimia ya kwamba ninyi (wapagani) mnaye Mercury (mungu-nyota wa Kirumi) wenu mnayemwabudu mkimwita Neno, mtumishi wa Mungu. . . . . Na kwa Yesu kuzaliwa na bikira, ninyi mnaye Perseus wenu kumlinganisha naye. . . . Kama Jupiter (mungu-nyota wa kipagani) aliweza kuleta kikundi cha wana waliozaliwa na mabikira; Baba wa mbinguni bila shaka angeweza kufanya hivyo angalau kwa ajili yetu" (Adol, I ch. xxii).

Jerome Mt. na mapadre wengine walishtushwa na kupatana huko, na kadhalika Cortez, aliyeivumbua Mexico alinung'unika ya kuwa Shetani aliwafunza Wamexico mambo yale yale ambayo Mungu aliwafunza Wakristo (Conquest of Mexico, vol. I. p. 60).

HALI YA WAPROTESTANTI.

Maneno hayo yanadhihirisha waziwazi ya kuwa Ukristo ulio leo ni upagani uliokuwa kwa washenzi wa zamani. Haya yote yanahusiana na Wakatoliki; lakini kwa kuwa dini ya Waprotestanti imewafikia toka mikono ya hao hao Wakatoliki, imelazimu sehemu ya upagani pia wawe wameichukua. Kwa mfano sikukuu ya Krismas; Dean Farrar katika kitabu chake "Life of Christ" ameeleza kwamba hakuna ushahidi unaoridhisha kwa kufanya tarehe 25 Desemba kuwa siku aliyozaliwa Yesu. Biblia haisemi neno juu ya jambo hili ingawa inaonyesha ya kwamba usiku ule wachungaji wa mifugo walikuwa pamoja na wanyama wao katika mashamba ya Bethlehem (Encyclopaedia of Religions and Ethics, art. "Christmas"). Inakuwa ni vigumu kukubali tarehe 25 Desemba kuwa ndio aliyozaliwa Yesu, maana majira hayo ni ya mvua kubwa katika Uyahudi, na isingewezekana wanyama na wachungaji kuwa nje wakati wa usiku.

SIKU KUU YA KRISMAS KWANZA ILIFANYWA JANUARI.

Uesener anasema ya kwamba sikukuu ya kuzaliwa Yesu hapo kwanza ilikuwa inafanywa tarehe 6 Januari ("Epiphany," yaani sikukuu ya kuonekana Yesu na Majusi). Lakini miaka 353 mpaka 354 baada ya Yesu, Pope Liberius akaihamishia kwenye tarehe 25 Desemba, lakini hakuna ushahidi wa sikukuu ya "Epiphany" kufanyika wakati wo wote kabla ya karne ya nne baada ya Yesu. Haikuwa ila katika mwaka wa 534, baada ya Yesu, ndipo sikukuu ya Krismas na ya "Epiphany" zilipokubaliwa na serikali kuwa sikukuu, na watu kupewa ruhusa wasiende kazi (Encyclopaedia of Rl. and Ethics, art "Christmas").

Mpaka hivi leo Kanisa la Kigiriki haliadhimishi sikukuu ya Krismas tarehe 25 Desemba, bali tarehe 7 Januari. Ilikuwa mwaka 530 au hivi, mmonaki wa Scythia aitwaye Dionysius Exiguus, ambaye alikuwa mnajimu (mwenye elimu ya nyota) na mkuu wa nyumba ya watawa, alipoambiwa aweke tarehe na mwaka aliozaliwa Yesu. Yeye ndiye aliyeweka hii tarehe 25 Desemba, bila kueleza sababu zilizomfikisha kwenye tarehe hiyo. Jambo ni kwamba tarehe hiyo siku moja au mbili ndio hudhaniwa kuzaliwa miungu-Jua wengi. Kwa kalenda ya mtawa wa Kirumi aliyeitwa Julius Caesar, tarehe hiyo 25 Desemba, ndio tarehe ya kuzaliwa Jua. Mithra, kama tulivyokwisha onyesha, alizaliwa tarehe hiyo hiyo. Mungu-Jua wa Wamisri aliyeitwa Osiris alizaliwa siku mbili baada ya tarehe hiyo, na kadhalika miungu-Jua wengine. Hivyo Wakristo walichukua tu tarehe hiyo kwa vile ilionekana itapatana na desturi walizozoea watu za sikukuu za kuzaliwa miungu ya wapagani.

اِتَّخَذُوْٓا اَحْبَارَهُمْ وَرُهْبَانَهُمْ اَرْبَابًا مِّنْ دُوْنِ اللّٰهِ وَالْمَسِيْحَ ابْنَ مَرْيَمَ ۚ وَمَآ اُمِرُوْٓا اِلَّا لِيَعْبُدُوْٓا اِلٰهًا وَّاحِدًا ۚ لَآ اِلٰهَ اِلَّا هُوَ ۭ سُبْحٰنَهٗ عَمَّا يُشْرِكُوْنَ ۝۳۱

31. Wamewafanya wanazuoni wao na watawa wao kuwa ni miungu badala ya Allah na Masihi mwana wa Mariamu pia (wamemfanya mungu); hali hawakuamrishwa isipokuwa kumwabudu Mungu Mmoja, hakuna aabudiwaye ila Yeye, Ametakasika na yale wanayomshirikisha nayo.

SIKUKUU YA KUTAKASWA BIKIRA.

Kadhalika sikukuu ya Kutakaswa Bikira iitwayo *Candlemas* imewekewa tarehe 2 Februari inayopatana na sikukuu kama hiyo ya kipagani iitwayo *Juno Februata* (Kutakaswa) iliyokuwa ikifanyika mwezi huo huo katika enzi ya Warumi, na watu wakiandamana wamechukua mishumaa.

Katika Alexandria kulikuwa kunaabudiwa mungu-Jua akiitwa Serapis, asemavyo Macrobius. Mfalme Hadrian aliandika barua kwa Servianus juu ya wenyeji wa Alexandria, na akasema, "hao wanaomwabudu Serapis pia ni Wakristo, hata hao wanaojiita maaskofu wa Kristo wanamwabudu Serapis" *(Vosipiacus vit. Saturninus).*

Huko Alexandria kulikuwa mungu-mama aitwaye Isis ambaye mwanamke Horus aliitwa Mwokozi karne nyingi kabla ya kufika Ukristo. Huyo Isis alikuwa akiabudiwa kwa jina la "Bibi Yetu," na "Malkia wa Mbinguni," ambayo ni majina aliyopewa Mariamu baadaye na Wakatoliki.

JUMAPILI KUFANYWA SABATO NI UPAGANI.

Kubadilishwa kwa Sabato ya Kiyahudi iliyoamrishwa katika amri kumi, toka Jumamosi kuitia katika Jumapili, pia ni jambo la kipagani. Mfalme Konstantino kabla hajaingia Ukristo alikuwa akimwabudu Apollo, mungu-Jua. Ingawa alingia Ukristo, muhuri wake ulidumu kuwa na chapa ya Apollo na uliandikwa "Kwa jua asiyeshindika Rafiki yangu." Konstantino hakwenda kinyume na dini ya jadi yao iliyopendelewa sana na watu. Kwake yeye jina la "Kristo" lilikuwa fani ya mungu-Jua. Makanisa ya kipagani aliyaweka imara yakiendesha ibada zao na kanuni zao. Siku ya Jumapili, kama tulivyokwisha sema, ndio ilikuwa akiabudiwa Jua, mungu mkuu wa Warumi. Ili kuwaheshimu Warumi waabudu-Jua, Konstantino asingefanya jambo zuri zaidi kuliko kuifanya hiyo hiyo Jumapili ya wapagani iwe Sabato ya Wakristo; nayo imedumu hata leo.

Huko Ulaya wachunguzi wengi walipoanza kufunua siri hizi za Kanisa, watu wameachilia mbali kufika makanisani. ila wachache tu. Ingekuwa vyema hawa mapadre wakaacha kwanza kueneza hii dini yao hapa, wawarudie jamaa zao wanaoponyoka, wasitake kwenda kuabudu jua kwa jina la Kristo. Sikukuu za Kikristo karibu zote zinahakikishwa na watu wenye elimu kuwa zimetokana na habari za jua. Falsafa (philosophy) ya dini yao ni ile ile ya mapagani wa zamani.

UKWELI WA QUR'AN UMETHIBITIKA.

Qur'an ilitaja jambo hili la watu hawa kuingiza katika dini yao fikira za makafiri wa zamani, toka miaka 1400 kabla ya mtu ye yote hajawaza jambo hili. Na sasa kuna vitabu vingi vimeandikwa na watu wa Ulaya juu ya jambo hili na wamehakikisha kabisa kuwa Ukristo huu si cho chote ila upagani. Je, siyo dhahiri ya kuwa Allah kwa kuwahurumia watu akaleta Qur'an pamoja na Mtume Muhammad s.a.w. kuonyesha watu njia. Ingekuwa vizuri kwa Wakristo kuangalia shauri hili.

Aya 31. *Wamewafanya wanazuoni na watawa wao kuwa miungu,* maana yake ni kuwatii kama inavyopasa kumtii Mungu. Kuna taifa moja katika Wakristo, wanaojiita shina la Ukristo, ambao wanadai na kutilia nguvu utakatifu wa "Kanisa." Hao wanafanya mambo mengi

32. Wanataka kuizima nuru ya Allah kwa vinywa vyao, lakini Allah Anakataa (jambo lingine lolote) isipokuwa kuitimiza nuru Yake, ijapokuwa makafiri wachukie.

يُرِيْدُوْنَ اَنْ يُّطْفِـُٔوْا نُوْرَ اللّٰهِ بِاَفْوَاهِهِمْ وَيَاْبَى اللّٰهُ اِلَّآ اَنْ يُّتِمَّ نُوْرَهٗ وَلَوْ كَرِهَ الْكٰفِرُوْنَ ﴿٣٢﴾

33. Yeye ndie Aliyemtuma Mtume Wake kwa mwongozo na dini ya haki ili Aishindishe juu ya dini zote, ijapokuwa washirikina wachukie.

هُوَ الَّذِيْٓ اَرْسَلَ رَسُوْلَهٗ بِالْهُدٰى وَدِيْنِ الْحَقِّ لِيُظْهِرَهٗ عَلَى الدِّيْنِ كُلِّهٖ ۙ وَلَوْ كَرِهَ الْمُشْرِكُوْنَ ﴿٣٣﴾ ع

34. Enyi mlioamini! bila shaka wengi katika makasisi na wamonaki wanakula mali za watu kwa batili na kuwazuilia njia ya Allah. Na wale wakusanyao dhahabu na fedha wala hawazitoi katika njia ya Allah, basi wape habari za adhabu iumizayo.

يٰٓاَيُّهَا الَّذِيْنَ اٰمَنُوْٓا اِنَّ كَثِيْرًا مِّنَ الْاَحْبَارِ وَالرُّهْبَانِ لَيَاْكُلُوْنَ اَمْوَالَ النَّاسِ بِالْبَاطِلِ وَيَصُدُّوْنَ عَنْ سَبِيْلِ اللّٰهِ ؕ وَالَّذِيْنَ يَكْنِزُوْنَ الذَّهَبَ وَالْفِضَّةَ وَلَا يُنْفِقُوْنَهَا فِيْ سَبِيْلِ اللّٰهِ ۙ فَبَشِّرْهُمْ بِعَذَابٍ اَلِيْمٍ ﴿٣٤﴾

yasiyoamrishwa na Yesu Kristo, kwa amri ya kanisa tu. kama kuangika msalaba shingoni, na kuacha kutumia nyama siku ya Ijumaa. Wamevunja amri ya talaka iliyotolewa na Yesu waziwazi (Mathayo5:32)Wanasema,"Iwapo watu wawili wametengana kwa ajili ya uzinifu,hata hivi ndoa haivunjiki"(Maelezo chini ya Mathayo5:32)Kwa kuondoa ruhusa ya talaka na ya kuoa mke wa pili, wamewasukuma Wakristo wengi katika uzinifu na usumbufu wa maisha.

Amri ya Sabato iliyoshikwa tangu miaka na miaka iligeuzwa kwa amri ya makasisi na mapadre. Ajabu ni hii ya kwamba hata Yesu hakutoa amri ya kuacha Jumamosi iliyo ni siku ya Sabato na kushika Jumapili badala yake. Katika kitabu kiitwacho, "Maandiko matakatifu yasemaje?" Padre Pittway ameeleza ya kwamba wamefanya hivi kwa sababu Yesu Kristo alifufuka siku ya Jumapili. Amekubali ya kwamba mapadre ndio waliobuni amri hiyo wenyewe wakawashurutisha Wakristo wengine washike fundisho lao kinyume na Biblia. Yesu alikaa na wafuasi wake siku arobaini baada ya kutoka 'kaburini' (Matendo 1:3), lakini hakuthubutu kugeuza siku iliyobarikiwa na Mungu (Mwanzo 2:3). Kwa sababu hizi na nyinginezo imesemwa ya kwamba wamewafanya wanazuoni wao kuwa miungu yao. Ama uungu wa Yesu, wanaukubali Wakristo karibu wote ingawa yeye alikuwa mwanadamu tu.

Aya 33. *Aishindishe juu ya dini zote.* Ahadi hii ni ya siku zote. Zamani Islam ilishinda dini zote na iliushinda Ukristo. Katika zama hizi pia ahadi hii itatimia maana Allah amemwinua Masihi Aliyeahidiwa, Mwanzishaji mtakatifu wa Mwendeleo wa Ahmadiyya, ili kuitumikia na kuiinua dini ya Kiislamu. Ushindi huu utakuwa kamili na utadumu kabisa. Kwa hakika mufasirina wengi (mathalan, Bayan) wanakubali ya kuwa ushindi wa mwisho na ulio kamilika wa ahadi hii iliyomo katika Aya hii utatokea wakati wa kufika Masihi Aliyeahidiwa.

Aya 34. Hapa imeelezwa dalili nyingine ya upotevu wa Wakristo. Injili ya Mathayo inasema, "Mmepata bure, toeni bure" (10:18). Kinyume kabisa na fundisho hili, mapadre walivumbua njia nyingine za kusomba mali za watu. Mapapa waliwauzia watu "Vyeti vya msamaha" wakisema ati Mkristo ambaye anacho cheti cha Papa atakaribishwa vizuri mbinguni. Wengine wao walizikwa pamoja na funguo za kufungulia vyumba vya Peponi.

يَّوْمَ يُحْمٰى عَلَيْهَا فِيْ نَارِ جَهَنَّمَ فَتُكْوٰى بِهَا
جِبَاهُهُمْ وَجُنُوْبُهُمْ وَظُهُوْرُهُمْ ؕ هٰذَا
مَا كَنَزْتُمْ لِاَنْفُسِكُمْ فَذُوْقُوْا مَا
كُنْتُمْ تَكْنِزُوْنَ ﴿٣٥﴾

35. Siku (mali yao) itakapochomwa ndani ya moto wa Jahanamu, na kwayo vitachomwa vipaji vya nyuso zao na mbavu zao na migongo yao: haya ndio mliyoyakusanyia nafsi zenu, basi onjeni (adhabu ya) yale mliyokuwa mkiyakusanya.

اِنَّ عِدَّةَ الشُّهُوْرِ عِنْدَ اللّٰهِ اثْنَا عَشَرَ
شَهْرًا فِيْ كِتٰبِ اللّٰهِ يَوْمَ خَلَقَ السَّمٰوٰتِ
وَالْاَرْضَ مِنْهَآ اَرْبَعَةٌ حُرُمٌ ؕ ذٰلِكَ
الدِّيْنُ الْقَيِّمُ ۙ فَلَا تَظْلِمُوْا فِيْهِنَّ
اَنْفُسَكُمْ وَقَاتِلُوا الْمُشْرِكِيْنَ كَآفَّةً
كَمَا يُقَاتِلُوْنَكُمْ كَآفَّةً ؕ وَاعْلَمُوْٓا اَنَّ
اللّٰهَ مَعَ الْمُتَّقِيْنَ ﴿٣٦﴾

36. Hakika idadi ya miezi mbele ya Allah ni miezi kumi na mbili ndani ya kitabu cha Allah tangu siku Alipoiumba mbingu na ardhi. Katika hiyo imo minne iliyo mitukufu; hii ndio dini yenye kudumu. Basi msijidhulumu nafsi zenu katika hiyo. Na nyote piganeni na washirikina kama wao wote wapiganavyo nanyi; na jueni kwamba Allah Yu pamoja na wamwogopao.

اِنَّمَا النَّسِيْٓءُ زِيَادَةٌ فِي الْكُفْرِ يُضَلُّ
بِهِ الَّذِيْنَ كَفَرُوْا يُحِلُّوْنَهٗ عَامًا
وَّ يُحَرِّمُوْنَهٗ عَامًا لِّيُوَاطِـُٔوْا عِدَّةَ مَا
حَرَّمَ اللّٰهُ فَيُحِلُّوْا مَا حَرَّمَ اللّٰهُ ؕ زُيِّنَ
لَهُمْ سُوْٓءُ اَعْمَالِهِمْ ؕ وَاللّٰهُ لَا يَهْدِي
الْقَوْمَ الْكٰفِرِيْنَ ﴿٣٧﴾ ع ١٣

37. Bila shaka kuahirisha (Miezi mitukufu) ni kuzidi katika kufuru; kwayo hupotezwa waliokufuru. Wanauhalalisha (Mwezi mtukufu) mwaka mmoja na kuuharamisha Mwaka mwingine ili wafanye kuwa sawa idadi ya ile Aliyoiharamisha Allah; hivyo huhalalisha Alivyoviharamisha Allah. Wamepambiwa ubaya wa vitendo vyao, na Allah Hawaongozi watu makafiri.

Katika nchi hii baadhi ya makanisa yameweka bei maalumu ya ubatizo, mtu asipate jina la Kikristo asipotoa bei kamili. Kusaidia dini ni jambo zuri sana. Lakini kushurutisha hivyo na kuiuza dini haisadikiki kwamba ni mapenzi ya Mungu. Ziko Sakramenti nyingine ambazo hununuliwa kwa shilingi nyingi. Yesu Kristo alisema, Ni vigumu tajiri kuingia ufalme wa mbinguni (Matei 19:23). Sasa mambo yamebadilika. Mwenye malundo ya mali ndiye anaweza kuwa Mkristo safi; na maskini ni vigumu kwake kuingia ufalme wa mbinguni. Mara nyingi mwenye kupokea sadaka (padre) huwa na utajiri mwingi kuliko aitoaye.

Waislamu ijapokuwa walionywa wasifuate nyayo za wale waliopotea kabla yao, lakini kwa masikitiko mengi baadhi ya masheikh na walimu wanakula mali za wenzao kwa udanganyifu, hasa kwa kuwauzia hirizi na talasimu, ambavyo ni vitu visivyo na maana.

Aya 37. *Kuahirisha.* Aya hii inaeleza desturi ya Waarabu ya kuahirisha miezi. Kuna miezi

FUNGU 6

يٰٓاَيُّهَا الَّذِيْنَ اٰمَنُوْا مَا لَكُمْ اِذَا قِيْلَ لَكُمُ انْفِرُوْا فِيْ سَبِيْلِ اللّٰهِ اثَّاقَلْتُمْ اِلَى الْاَرْضِ ؕ اَرَضِيْتُمْ بِالْحَيٰوةِ الدُّنْيَا مِنَ الْاٰخِرَةِ ۚ فَمَا مَتَاعُ الْحَيٰوةِ الدُّنْيَا فِي الْاٰخِرَةِ اِلَّا قَلِيْلٌ ﴿٣٨﴾

38. Enyi mlioamini! mmekuwaje mnapoambiwa, nendeni (kupigana) katika njia ya Allah mnajitia uzito katika ardhi? Je, mmekuwa radhi na maisha ya dunia kuliko ya Akhera? Lakini manufaa ya maisha ya dunia mbele ya Akhera ni kidogo tu.

اِلَّا تَنْفِرُوْا يُعَذِّبْكُمْ عَذَابًا اَلِيْمًا ۙ وَّيَسْتَبْدِلْ قَوْمًا غَيْرَكُمْ وَلَا تَضُرُّوْهُ شَيْـًٔا ؕ وَاللّٰهُ عَلٰى كُلِّ شَيْءٍ قَدِيْرٌ ﴿٣٩﴾

39. Mkikosa kwenda Atawaadhibuni kwa adhabu iumizayo, na Atawaleta watu wengine badala yenu, wala hamtamdhuru cho chote; na Allah ni Mweza juu ya kila kitu.

اِلَّا تَنْصُرُوْهُ فَقَدْ نَصَرَهُ اللّٰهُ اِذْ اَخْرَجَهُ الَّذِيْنَ كَفَرُوْا ثَانِيَ اثْنَيْنِ اِذْ هُمَا فِي الْغَارِ اِذْ يَقُوْلُ لِصَاحِبِهٖ لَا تَحْزَنْ اِنَّ اللّٰهَ مَعَنَا ۚ فَاَنْزَلَ اللّٰهُ سَكِيْنَتَهٗ عَلَيْهِ وَاَيَّدَهٗ بِجُنُوْدٍ لَّمْ تَرَوْهَا وَجَعَلَ كَلِمَةَ الَّذِيْنَ كَفَرُوا السُّفْلٰى ؕ وَكَلِمَةُ اللّٰهِ هِيَ الْعُلْيَا ؕ وَاللّٰهُ عَزِيْزٌ حَكِيْمٌ ﴿٤٠﴾

40. Kama hamtamsaidia, basi Allah Amekwisha msaidia walipomtoa wale waliokufuru; alipokuwa wa pili katika wawili, walipokuwa wote wawili katika pango, alipomwambia sahibu yake: Usihuzunike, kwa yakini Allah Yu pamoja nasi. Ndipo Allah Akamteremshia utulivu Wake, na Akamsaidia kwa majeshi msiyoyaona, na Akafanya neno la wale waliokufuru kuwa chini; na neno la Allah ndilo la juu. Na Allah ndiye Ashindaye. Mwenye hekima.

---

mitatu mitakatifu inayofuatana ambayo kupigana na kufanya ghasia katika hiyo ni haramu kabisa, na Waarabu wote toka siku za ujahili walitii sheria hii. Miezi hiyo ni *Dhul-Qaada, Dhul-Hijja* na *Muharram.* Wakati mwingine muda huu ulionekana mrefu mno kwa Waarabu, wakitaka kwenda nyang'anya. Basi wanafanya hila moja, mwezi ulio mtakatifu wanaufanya ni wa desturi tu na mwezi mwingine wa desturi wanaufanya mtakatifu. Desturi hii Allah anailaumu maana iliharibu usalama wa maisha ambao ulihifadhiwa katika miezi hiyo.

Aya 40. Aya hii inaeleza habari za kuhama Mtume s.a.w kutoka Makka kwenda Madina pamoja na Seyidna Abu Bakar na wakajificha katika pango linaloitwa Thaur. Hapa utukufu wa Abu Bakar umeonyeshwa na Allah mwenyewe. Wafuasi wa Nabii Musa walipokuwa katika wasiwasi, Musa akawaambia, *Mola wangu yu pamoja nami, bila shaka Ataniongoza* (sura 26:62,63).

41. Nendeni mkiwa mmesheheni silaha au la na fanyeni jihadi kwa mali zenu na nafsi zenu katika njia ya Allah; hayo ni bora kwenu, ikiwa ninyi mnajua.

اِنْفِرُوْا خِفَافًا وَّ ثِقَالًا وَّ جَاهِدُوْا بِاَمْوَالِكُمْ وَاَنْفُسِكُمْ فِيْ سَبِيْلِ اللّٰهِ ؕ ذٰلِكُمْ خَيْرٌ لَّكُمْ اِنْ كُنْتُمْ تَعْلَمُوْنَ ﴿۴۱﴾

42. Kama ingalikuwa faida ya papo kwa papo na safari iliyo fupi, kwa yakini wangalikufuata; lakini safari ya taabu imekuwa ndefu kwao. Nao wataapa kwa Allah, kama tungaliweza bila shaka tungalitoka pamoja nanyi. Wanaangamiza nafsi zao; na Allah Anajua kwa hakika wao ni waongo tu.

لَوْ كَانَ عَرَضًا قَرِيْبًا وَّسَفَرًا قَاصِدًا لَّاتَّبَعُوْكَ وَلٰكِنْۢ بَعُدَتْ عَلَيْهِمُ الشُّقَّةُ ؕ وَسَيَحْلِفُوْنَ بِاللّٰهِ لَوِ اسْتَطَعْنَا لَخَرَجْنَا مَعَكُمْ ۚ يُهْلِكُوْنَ اَنْفُسَهُمْ ۚ وَاللّٰهُ يَعْلَمُ اِنَّهُمْ لَكٰذِبُوْنَ ﴿۴۲﴾ ع

FUNGU 7

43. Allah Akusamehe! Kwa nini umewapa ruhusa? (Ungengoja) mpaka wanaosema kweli wangekupambanukia, na ungaliwajua waongo.

عَفَا اللّٰهُ عَنْكَ ۚ لِمَ اَذِنْتَ لَهُمْ حَتّٰى يَتَبَيَّنَ لَكَ الَّذِيْنَ صَدَقُوْا وَتَعْلَمَ الْكٰذِبِيْنَ ﴿۴۳﴾

44. Hawatakuomba ruhusa wale wanaomuamini Allah na Siku ya Mwisho kwamba wasijitahidi kwa mali zao na nafsi zao. na Allah Awajua wanaomcha.

لَا يَسْتَاْذِنُكَ الَّذِيْنَ يُؤْمِنُوْنَ بِاللّٰهِ وَالْيَوْمِ الْاٰخِرِ اَنْ يُّجَاهِدُوْا بِاَمْوَالِهِمْ وَاَنْفُسِهِمْ ؕ وَاللّٰهُ عَلِيْمٌۢ بِالْمُتَّقِيْنَ ﴿۴۴﴾

45. Hakika wanakuomba ruhusa wale tu wasiomuamini Allah na siku ya Mwisho, na mioyo yao ina shaka, kwa hiyo wanasitasita katika shaka yao.

اِنَّمَا يَسْتَاْذِنُكَ الَّذِيْنَ لَا يُؤْمِنُوْنَ بِاللّٰهِ وَالْيَوْمِ الْاٰخِرِ وَارْتَابَتْ قُلُوْبُهُمْ فَهُمْ فِيْ رَيْبِهِمْ يَتَرَدَّدُوْنَ ﴿۴۵﴾

46. Na kama wangalitaka kutoka bila shaka wangaliiandalia maandalio; lakini Allah Hakupenda kutoka kwao. Na kwa

وَلَوْ اَرَادُوا الْخُرُوْجَ لَاَعَدُّوْا لَهٗ عُدَّةً وَّلٰكِنْ كَرِهَ اللّٰهُ انْۢبِعَاثَهُمْ فَثَبَّطَهُمْ

Lakini maadui walipokaribia mahali Mtume na Seyidna Abu Bakar walipojificha, Seyidna Abu Bakar akapata huzuni, Mtume s.a.w alimwambia, "Usihuzunike, kwa yakini Allah yu pamoja nasi." Hakusema yu pamoja nami, bali pamoja nasi sote wawili. Tena walipokuwa pangoni Seyidna Abu Bakar alianza kutoa machozi, na Mtume akamwuliza kwa nini analia. Akajibu, "Mimi sililii uzima wangu, maana nikifa, nimekufa mtu mmoja. Lakini ukifa wewe, Ee Mtume wa Mungu, itakuwa kifo cha Uislamu na kifo cha wote" (Zurakani).

Aya 43. *'Afallaahu 'anka.* "Allah akuwie radhi." Waarabu wanatumia kwa kumwambia mtu aliye na heshima sana, *'Afallaahu 'anka,* kwa maana ya kwamba Allah akuongozee mambo yako na akupe heshima na utukufu (Akrab).

وَقِيْلَ اقْعُدُوْا مَعَ الْقٰعِدِيْنَ ﴿٤٦﴾

hiyo Akawazuia na ikasemwa: Bakieni pamoja na wabakiao.

لَوْ خَرَجُوْا فِيْكُمْ مَّا زَادُوْكُمْ اِلَّا خَبَالًا وَّلَاْ اَوْضَعُوْا خِلٰلَكُمْ يَبْغُوْنَكُمُ الْفِتْنَةَ ۚ وَفِيْكُمْ سَمّٰعُوْنَ لَهُمْ ؕ وَاللّٰهُ عَلِيْمٌۢ بِالظّٰلِمِيْنَ ﴿٤٧﴾

47. Kama wangalitoka pamoja nanyi wasingaliwazidishieni ila machafuko na wangeharakia huko na huko kati yenu kuwatakieni fitina. Na miongoni mwenu wako wanaowasikilizia. Na Allah Anawajua wadhalimu.

لَقَدِ ابْتَغَوُا الْفِتْنَةَ مِنْ قَبْلُ وَقَلَّبُوْا لَكَ الْاُمُوْرَ حَتّٰى جَآءَ الْحَقُّ وَظَهَرَ اَمْرُ اللّٰهِ وَهُمْ كٰرِهُوْنَ ﴿٤٨﴾

48. Bila shaka zamani walitaka fitina na wakakupindulia mambo mpaka ikafika haki na kudhihirika amri ya Allah ingawa wamechukia.

وَمِنْهُمْ مَّنْ يَّقُوْلُ ائْذَنْ لِّيْ وَلَا تَفْتِنِّيْ ؕ اَلَا فِي الْفِتْنَةِ سَقَطُوْا ؕ وَاِنَّ جَهَنَّمَ لَمُحِيْطَةٌۢ بِالْكٰفِرِيْنَ ﴿٤٩﴾

49. Na miongoni mwao yuko asemaye: Niruhusu, wala usinitie katika fitina. Hakika wao wameanguka katika fitina. Na kwa hakika Jahanamu ndio iwazungukayo makafiri.

اِنْ تُصِبْكَ حَسَنَةٌ تَسُؤْهُمْ ۚ وَاِنْ تُصِبْكَ مُصِيْبَةٌ يَّقُوْلُوْا قَدْ اَخَذْنَاۤ اَمْرَنَا مِنْ قَبْلُ وَيَتَوَلَّوْا وَّهُمْ فَرِحُوْنَ ﴿٥٠﴾

50. Kama ukikufikia wema unawachukiza; na kama ukikufikia msiba, husema: Hakika tuliangalia zamani mambo yetu, na hukengeuka huku wanafurahia.

قُلْ لَّنْ يُّصِيْبَنَاۤ اِلَّا مَا كَتَبَ اللّٰهُ لَنَا ۚ هُوَ مَوْلٰىنَا ۚ وَعَلَى اللّٰهِ فَلْيَتَوَكَّلِ الْمُؤْمِنُوْنَ ﴿٥١﴾

51. Sema: Hautatusibu kamwe ila aliotuandikia Allah. Yeye ni Mola wetu, basi waaminio wamtegemee Allah.

قُلْ هَلْ تَرَبَّصُوْنَ بِنَاۤ اِلَّاۤ اِحْدَى الْحُسْنَيَيْنِ ؕ وَنَحْنُ نَتَرَبَّصُ بِكُمْ اَنْ يُّصِيْبَكُمُ اللّٰهُ بِعَذَابٍ مِّنْ عِنْدِهٖۤ اَوْ بِاَيْدِيْنَا ۚ فَتَرَبَّصُوْۤا اِنَّا مَعَكُمْ مُّتَرَبِّصُوْنَ ﴿٥٢﴾

52. Sema: Ninyi hamtutazamii ila (kupata) moja katika mema mawili. Nasi tunawatazamieni kwamba Allah Awafikishieni adhabu itokayo Kwake au kwa mikono yetu. Basi ngojeni, nasi tunangoja pamoja nanyi.

قُلْ اَنْفِقُوْا طَوْعًا اَوْ كَرْهًا لَّنْ يُّتَقَبَّلَ مِنْكُمْ ؕ اِنَّكُمْ كُنْتُمْ قَوْمًا فٰسِقِيْنَ ﴿٥٣﴾

53. Sema: Toeni kwa kupenda au kwa kutopenda, haitakubaliwa kwenu. Hakika ninyi ni watu waasi.

54. Na haikuwazuia ikubaliwe kwao michango yao, ila ya kwamba walimkataa Allah na Mtume Wake, wala hawafiki kusali ila huwa wavivu, wala hawatoi ila huwa wamechukia.

وَمَا مَنَعَهُمْ اَنْ تُقْبَلَ مِنْهُمْ نَفَقٰتُهُمْ اِلَّآ اَنَّهُمْ كَفَرُوْا بِاللّٰهِ وَبِرَسُوْلِهٖ وَلَا يَاْتُوْنَ الصَّلٰوةَ اِلَّا وَهُمْ كُسَالٰى وَلَا يُنْفِقُوْنَ اِلَّا وَهُمْ كٰرِهُوْنَ ﴿٥٤﴾

55. Basi zisikustaajabishe mali zao wala watoto wao; hakika Allah Anataka kuwaadhibu kwayo katika maisha ya dunia, na roho zao zitoke hali ya kuwa makafiri.

فَلَا تُعْجِبْكَ اَمْوَالُهُمْ وَلَآ اَوْلَادُهُمْ ؕ اِنَّمَا يُرِيْدُ اللّٰهُ لِيُعَذِّبَهُمْ بِهَا فِى الْحَيٰوةِ الدُّنْيَا وَتَزْهَقَ اَنْفُسُهُمْ وَهُمْ كٰفِرُوْنَ ﴿٥٥﴾

56. Na wanaapa kwa Allah ya kwamba wao ni pamoja nanyi, hali wao si pamoja nanyi, bali wao ni watu waoga.

وَيَحْلِفُوْنَ بِاللّٰهِ اِنَّهُمْ لَمِنْكُمْ ؕ وَمَا هُمْ مِّنْكُمْ وَلٰكِنَّهُمْ قَوْمٌ يَّفْرَقُوْنَ ﴿٥٦﴾

57. Kama wangalipata kimbilio au mapango au mahali pengine pa kuingia, bila shaka wangaligeukia huko wakikimbia.

لَوْ يَجِدُوْنَ مَلْجَاً اَوْ مَغٰرٰتٍ اَوْ مُدَّخَلًا لَّوَلَّوْا اِلَيْهِ وَهُمْ يَجْمَحُوْنَ ﴿٥٧﴾

58. Na miongoni mwao yuko anayekusingizia kuhusiana na sadaka. Na kama wakipewa katika hiyo, huridhika; na kama wasipopewa katika hiyo, hapo hukasirika.

وَمِنْهُمْ مَّنْ يَّلْمِزُكَ فِى الصَّدَقٰتِ ۚ فَاِنْ اُعْطُوْا مِنْهَا رَضُوْا وَاِنْ لَّمْ يُعْطَوْا مِنْهَآ اِذَا هُمْ يَسْخَطُوْنَ ﴿٥٨﴾

59. Na kama wangeyaridhia yale aliyowapa Allah na Mtume Wake, na wakasema: Allah Anatutosha, Bila shaka Allah Atatupa katika fadhili Zake na pia Mtume Wake; Hakika sisi tunaelekea kwa Allah.

وَلَوْ اَنَّهُمْ رَضُوْا مَآ اٰتٰىهُمُ اللّٰهُ وَرَسُوْلُهٗ ۙ وَقَالُوْا حَسْبُنَا اللّٰهُ سَيُؤْتِيْنَا اللّٰهُ مِنْ فَضْلِهٖ وَرَسُوْلُهٗٓ ۙ اِنَّآ اِلَى اللّٰهِ رٰغِبُوْنَ ﴿٥٩﴾ ع

Aya 54. Kazi nzuri zinakuwa namna mbili: (1) Zinazofanywa kwa ajili ya mtu kutakasa nafsi yake mwenyewe, na katika hizo Sala ni kubwa zaidi, na (2) zinazofanywa kwa ajili ya kuinua hali ya Jumuiya, na katika hizo Zaka na michango ya namna hiyo ndio kubwa. Aya inasema, wanafiki huwa wavivu na wasiopendelea haya yote mawili.

Aya 58. Wanafiki waliingia dini ya Kiislamu ili wapate faida za kidunia, basi walipopewa cho chote katika Zaka walionyesha furaha, lakini kama hawakupewa cho chote walinung'unika na kuanza kumlaumu Mtume s.a.w. Hii ni alama ya wazi kabisa ya wanafiki.

FUNGU 8

60. Sadaka ni kwa mafakiri tu na maskini na wanaozitumikia na waungiwao mioyo yao na (kwa kuwakomboa) wafungwa na wenye deni na katika njia ya Allah na msafiri. Ni faradhi kutoka kwa Allah; na Allah ni Mjuzi, Mwenye hekima.

إِنَّمَا الصَّدَقٰتُ لِلْفُقَرَآءِ وَالْمَسٰكِيْنِ وَالْعٰمِلِيْنَ عَلَيْهَا وَالْمُؤَلَّفَةِ قُلُوْبُهُمْ وَفِي الرِّقَابِ وَالْغٰرِمِيْنَ وَفِيْ سَبِيْلِ اللّٰهِ وَابْنِ السَّبِيْلِ ؕ فَرِيْضَةً مِّنَ اللّٰهِ ؕ وَاللّٰهُ عَلِيْمٌ حَكِيْمٌ ﴿٦٠﴾

61. Na miongoni mwao wako wanaomuudhi Nabii na wanasema: Yeye ni msikivu sana. Sema: Kupenda kwake kuwasikiliza watu wote ni jambo jema kwenu; anamwamini Allah na anawasadiki waaminio, na ni rehema kwa wale wanaoamini. Lakini wale wanaomuudhi Mtume wa Allah watakuwa na adhabu iumizayo.

وَمِنْهُمُ الَّذِيْنَ يُؤْذُوْنَ النَّبِيَّ وَيَقُوْلُوْنَ هُوَ اُذُنٌ ؕ قُلْ اُذُنُ خَيْرٍ لَّكُمْ يُؤْمِنُ بِاللّٰهِ وَيُؤْمِنُ لِلْمُؤْمِنِيْنَ وَرَحْمَةٌ لِّلَّذِيْنَ اٰمَنُوْا مِنْكُمْ ؕ وَالَّذِيْنَ يُؤْذُوْنَ رَسُوْلَ اللّٰهِ لَهُمْ عَذَابٌ اَلِيْمٌ ﴿٦١﴾

Aya 60. Aya hii inaeleza Zaka itumiwe namna gani; na zimetajwa njia nne: Kuwapa (1) mafukara, yaani maskini waliovunjwa na umaskini au na ugonjwa; (2) maskini, yaani wenye shida, wasio na kitu; (3) wafanyao kazi ya kukusanya Zaka; (4) waungiwao mioyo yao, yaani watu ambao nyoyo zao zimeelekea kwenye dini, lakini kwa kuwa wametengana na watu wao, wanakuwa na haja ya msaada wa pesa; na kadhalika watu wapya katika dini; (5) kuwakomboa wafungwa na watumwa; (6) wasio na uwezo wa kulipa madeni yao au waliopata hasara nzito katika biashara zao; (7) kwa kazi njema alizoamrisha Allah; na (8) wasafiri wanaopata taabu katika safari kwa kupungukiwa pesa au wanaosafiri kutafuta elimu, au kwa kutengeneza hali njema ya watu. Pia tazama sura 2:178.

Padre Dale amechukizwa na uzuri wa mafundisho hayo. Anasema, "Ni vigumu kusadiki ya kuwa mtu atapata imani iliyo thabiti, safi, kwa kupewa mateka ya vita" (Tafsiri yake uk. 605).

Kwanza Aya hii haihusiani na mateka. Bwana Dale ameifasiri Aya hii Hivi, "Sadaka wapewe maskini na fakiri tu, na wazichungao, na wale ambao mioyo yao imeungwa (na dini ya Islamu)" (uk. 178). Hakuna habari za mateka.

Tena Aya haisemi kwamba mali zitampa mtu imani safi, la. Kama tulivyokwisha eleza mbele, wale tu ambao wanavutwa na mafundisho ya Kiislamu, lakini wamepatikana na taabu nyingi kwa sababu ya kujiunga na Uislamu ndio wanaostahiki kusaidiwa.

Labda Wakristo hawasaidiani. Lakini Uislamu unazo njia nzuri za kuchukua mali kwa matajiri na kuzigawanyia maskini na wenye shida. Ndio kuondoa taabu duniani na kuleta usawa katika maisha ya watu iwezekanavyo.

Twaona watu wengi wanakubali dini ya Kikristo kwa tamaa ya mali, mafundisho ya kidunia, na vyeo vikubwa. Wengine wanatibiwa vizuri katika hospitali kwa sababu wanalo jina la Kikristo. Watu wenye tabia kama hiyo walimfuata Yesu kwa wingi. Mwenyewe alisema: "Nawaambieni hakika, ninyi mnanitafuta siyo kwa ajili ya kuona miujiza, lakini kwa sababu mmepata chakula mmeshiba." (Yohana 6:26),maana Yesu aliwaongezea chakula wakala wote wakashiba. Hao ndio waliomwacha Yesu peke yake walipomwona akitafutwa na maaskari, ingawa walijidai zamani kwamba, 'tutakufa pamoja nawe'.

يَحْلِفُوْنَ بِاللّٰهِ لَكُمْ لِيُرْضُوْكُمْ ۚ وَاللّٰهُ وَرَسُوْلُهٗۤ اَحَقُّ اَنْ يُّرْضُوْهُ اِنْ كَانُوْا مُؤْمِنِيْنَ ﴿٦٢﴾

62. Wanawaapieni Allah ili kuwaridhisheni; hali Allah, na pia Mtume Wake, Ana haki zaidi ya kuwa wao wamridhishe, ikiwa wao ni waaminio.

اَلَمْ يَعْلَمُوْۤا اَنَّهٗ مَنْ يُّحَادِدِ اللّٰهَ وَرَسُوْلَهٗ فَاَنَّ لَهٗ نَارَ جَهَنَّمَ خَالِدًا فِيْهَا ؕ ذٰلِكَ الْخِزْيُ الْعَظِيْمُ ﴿٦٣﴾

63. Je, hawajui ya kwamba anayefanya uadui na Allah na Mtume Wake, basi kwa ajili yake kuna moto wa Jahannam ambamo atakaa kwa muda mrefu? Hiyo ndio fedheha kubwa.

يَحْذَرُ الْمُنٰفِقُوْنَ اَنْ تُنَزَّلَ عَلَيْهِمْ سُوْرَةٌ تُنَبِّئُهُمْ بِمَا فِيْ قُلُوْبِهِمْ ؕ قُلِ اسْتَهْزِءُوْا ۚ اِنَّ اللّٰهَ مُخْرِجٌ مَّا تَحْذَرُوْنَ ﴿٦٤﴾

64. Wanafiki wanaogopa kuteremshiwa sura iwaambiayo yaliyomo katika mioyo yao. Sema: Fanyeni mzaha, hakika Allah Atayadhihirisha mnayoyaogopa.

وَلَئِنْ سَاَلْتَهُمْ لَيَقُوْلُنَّ اِنَّمَا كُنَّا نَخُوْضُ وَنَلْعَبُ ؕ قُلْ اَبِاللّٰهِ وَاٰيٰتِهٖ وَرَسُوْلِهٖ كُنْتُمْ تَسْتَهْزِءُوْنَ ﴿٦٥﴾

65. Na kama ukiwauliza, lazima watasema: Sisi tulikuwa tukidhihaki na kucheza tu. Sema: Je, mlikuwa mkimfanyia mzaha Allah na Aya Zake na Mtume wake?

لَا تَعْتَذِرُوْا قَدْ كَفَرْتُمْ بَعْدَ اِيْمَانِكُمْ ؕ اِنْ نَّعْفُ عَنْ طَآئِفَةٍ مِّنْكُمْ نُعَذِّبْ طَآئِفَةً ۢ بِاَنَّهُمْ كَانُوْا مُجْرِمِيْنَ ﴿٦٦﴾

66. Msitoe udhuru; hakika mmekwisha kufuru baada ya kuamini kwenu; kama Tukilisamehe kundi miongoni mwenu Tutaliadhibu kundi (jingine) kwa sababu wao walikuwa wakosefu.

FUNGU 9

اَلْمُنٰفِقُوْنَ وَالْمُنٰفِقٰتُ بَعْضُهُمْ مِّنْۢ بَعْضٍ ۘ يَاْمُرُوْنَ بِالْمُنْكَرِ وَيَنْهَوْنَ عَنِ الْمَعْرُوْفِ وَيَقْبِضُوْنَ اَيْدِيَهُمْ ؕ نَسُوا اللّٰهَ فَنَسِيَهُمْ ؕ اِنَّ الْمُنٰفِقِيْنَ هُمُ الْفٰسِقُوْنَ ﴿٦٧﴾

67. Wanaume wanafiki na wanawake wanafiki wanahusiana wao kwa wao; huyaamuru yaliyo mabaya na huyakataza yaliyo mazuri, na huifumba mikono yao (hufanya ubahili); wamemsahau Allah, basi Yeye pia Amewasahau; hakika wanafiki ndio wavunjao amri.

وَعَدَ اللّٰهُ الْمُنٰفِقِيْنَ وَالْمُنٰفِقٰتِ وَالْكُفَّارَ نَارَ جَهَنَّمَ خٰلِدِيْنَ فِيْهَا ؕ هِيَ حَسْبُهُمْ ۚ وَلَعَنَهُمُ اللّٰهُ ۚ وَلَهُمْ عَذَابٌ مُّقِيْمٌ ﴿٦٨﴾

68. Allah Amewaahidi wanafiki wanaume na wanafiki wanawake na makafiri moto wa Jahanamu kukaa humo. Huo unawatosha; na Allah Amewalaani; nao wana adhabu ikaayo.

كَالَّذِيْنَ مِنْ قَبْلِكُمْ كَانُوْٓا اَشَدَّ مِنْكُمْ قُوَّةً
وَّاَكْثَرَ اَمْوَالًا وَّاَوْلَادًا ؕ فَاسْتَمْتَعُوْا
بِخَلَاقِهِمْ فَاسْتَمْتَعْتُمْ بِخَلَاقِكُمْ كَمَا
اسْتَمْتَعَ الَّذِيْنَ مِنْ قَبْلِكُمْ بِخَلَاقِهِمْ
وَخُضْتُمْ كَالَّذِيْ خَاضُوْا ؕ اُولٰٓئِكَ
حَبِطَتْ اَعْمَالُهُمْ فِي الدُّنْيَا وَالْاٰخِرَةِ ۚ
وَاُولٰٓئِكَ هُمُ الْخٰسِرُوْنَ ﴿٦٩﴾

69. Sawa na wale waliokuwa kabla yenu, walikuwa wenye nguvu zaidi kuliko ninyi na wenye mali nyingi na watoto. Basi walinufaika na sehemu yao na ninyi mmenufaika na sehemu yenu kama walivyonufaika na sehemu yao wale waliokuwa kabla yenu; na mkaongea maneno ya upuuzi kama walivyoongea wao. Hao ndio vitendo vyao vimeharibika katika dunia na Akhera; na hao ndio wapatao hasara.

اَلَمْ يَاْتِهِمْ نَبَاُ الَّذِيْنَ مِنْ قَبْلِهِمْ قَوْمِ
نُوْحٍ وَّ عَادٍ وَّ ثَمُوْدَ ۬ۙ وَقَوْمِ اِبْرٰهِيْمَ
وَاَصْحٰبِ مَدْيَنَ وَالْمُؤْتَفِكٰتِ ؕ اَتَتْهُمْ
رُسُلُهُمْ بِالْبَيِّنٰتِ ۚ فَمَا كَانَ اللّٰهُ
لِيَظْلِمَهُمْ وَلٰكِنْ كَانُوْٓا اَنْفُسَهُمْ
يَظْلِمُوْنَ ﴿٧٠﴾

70. Je! hazikuwafikia habari za wale waliokuwa kabla yao watu wa Nuhu na 'Adi na Thamudi, na watu wa Ibrahimu, na wenyeji wa Madiani, na miji iliyopinduliwa? Mitume wao waliwafikia kwa Ishara waziwazi; basi Allah Hakuwa Mwenye kuwadhulumu, bali wao walikuwa wakijidhulumu wenyewe.

وَالْمُؤْمِنُوْنَ وَالْمُؤْمِنٰتُ بَعْضُهُمْ اَوْلِيَآءُ
بَعْضٍ ۘ يَاْمُرُوْنَ بِالْمَعْرُوْفِ وَيَنْهَوْنَ
عَنِ الْمُنْكَرِ وَيُقِيْمُوْنَ الصَّلٰوةَ وَيُؤْتُوْنَ
الزَّكٰوةَ وَيُطِيْعُوْنَ اللّٰهَ وَرَسُوْلَهٗ ؕ
اُولٰٓئِكَ سَيَرْحَمُهُمُ اللّٰهُ ؕ اِنَّ اللّٰهَ
عَزِيْزٌ حَكِيْمٌ ﴿٧١﴾

71. Na waaminio wanaume na waaminio wanawake ni marafiki wao kwa wao. Huyaamuru yaliyo mema na huyakataza yaliyo mabaya, na husimamisha Sala na hutoa Zaka na humtii Allah na Mtume Wake; hao ndio karibuni Allah Atawarehemu. Hakika Allah ni Mwenye nguvu, Mwenye hekima.

وَعَدَ اللّٰهُ الْمُؤْمِنِيْنَ وَالْمُؤْمِنٰتِ جَنّٰتٍ
تَجْرِيْ مِنْ تَحْتِهَا الْاَنْهٰرُ خٰلِدِيْنَ فِيْهَا
وَمَسٰكِنَ طَيِّبَةً فِيْ جَنّٰتِ عَدْنٍ ؕ
وَرِضْوَانٌ مِّنَ اللّٰهِ اَكْبَرُ ؕ ذٰلِكَ هُوَ
الْفَوْزُ الْعَظِيْمُ ﴿٧٢﴾ ع

72. Allah Amewaahidi waaminio wanaume na waaminio wanawake Bustani zipitazo mito ndani yao kukaa humo, na makao mazuri katika Bustani zenye kudumu; na radhi za Allah ndizo kubwa mno. Huo ndio ufaulu mkuu.

FUNGU 10

73. Ewe Nabii, shindana na makafiri na wanafiki na uwe mgumu kwao, na makazi yao ni Jahanamu, nayo ni marejeo mabaya.

يَٰٓأَيُّهَا ٱلنَّبِيُّ جَٰهِدِ ٱلْكُفَّارَ وَٱلْمُنَٰفِقِينَ وَٱغْلُظْ عَلَيْهِمْ ۚ وَمَأْوَىٰهُمْ جَهَنَّمُ ۖ وَبِئْسَ ٱلْمَصِيرُ ﴿٧٣﴾

74. Wanaapa kwa Allah (ya kwamba) hawakusema, na hakika wamekwishasema neno la kufuru, na wakakufuru baada ya Uislamu wao, na wakaazimia wasioweza kuyafikia. Na hawakuwachukia (waaminio) ila tu kwa sababu Allah na mtume Wake wamewatajirisha kwa Fadhili Yake. Kwa hiyo kama wakitubu itakuwa heri kwao; lakini kama wakigeuka, Allah Atawaadhibu kwa adhabu iumizayo katika dunia na Akhera; na hawatakuwa na rafiki wala msaidizi ardhini.

يَحْلِفُونَ بِٱللَّهِ مَا قَالُوا۟ ۗ وَلَقَدْ قَالُوا۟ كَلِمَةَ ٱلْكُفْرِ وَكَفَرُوا۟ بَعْدَ إِسْلَٰمِهِمْ وَهَمُّوا۟ بِمَا لَمْ يَنَالُوا۟ ۚ وَمَا نَقَمُوٓا۟ إِلَّآ أَنْ أَغْنَىٰهُمُ ٱللَّهُ وَرَسُولُهُۥ مِن فَضْلِهِۦ ۚ فَإِن يَتُوبُوا۟ يَكُ خَيْرًا لَّهُمْ ۖ وَإِن يَتَوَلَّوْا۟ يُعَذِّبْهُمُ ٱللَّهُ عَذَابًا أَلِيمًا ۙ فِى ٱلدُّنْيَا وَٱلْءَاخِرَةِ ۚ وَمَا لَهُمْ فِى ٱلْأَرْضِ مِن وَلِىٍّ وَلَا نَصِيرٍ ﴿٧٤﴾

75. Na miongoni mwao wako waliomwahidi Allah: Akitupa katika fadhili Zake, bila shaka tutatoa sadaka na lazima tutakuwa miongoni mwa watendao mema.

وَمِنْهُم مَّنْ عَٰهَدَ ٱللَّهَ لَئِنْ ءَاتَىٰنَا مِن فَضْلِهِۦ لَنَصَّدَّقَنَّ وَلَنَكُونَنَّ مِنَ ٱلصَّٰلِحِينَ ﴿٧٥﴾

76. Lakini Alipowapa katika fadhili Zake, wakayafanyia ubahili na wakageuka, nao ndio wakengeukao.

فَلَمَّآ ءَاتَىٰهُم مِّن فَضْلِهِۦ بَخِلُوا۟ بِهِۦ وَتَوَلَّوا۟ وَّهُم مُّعْرِضُونَ ﴿٧٦﴾

77. Kwa hiyo Akawaadhibu kwa kutia unafiki mioyoni mwao mpaka siku ya kukutana naye kwa sababu ya kumhalifu Allah ahadi waliyomwahidi, na kwa sababu walikuwa wanasema uwongo.

فَأَعْقَبَهُمْ نِفَاقًا فِى قُلُوبِهِمْ إِلَىٰ يَوْمِ يَلْقَوْنَهُۥ بِمَآ أَخْلَفُوا۟ ٱللَّهَ مَا وَعَدُوهُ وَبِمَا كَانُوا۟ يَكْذِبُونَ ﴿٧٧﴾

Aya 73. *Uwe mgumu kwao*, yaani usiwe tena laini kwa wanafiki au kuwahurumia kwa makosa yao kama ulivyowafanyia zamani, bali sasa kila wakikosa waitwe kueleza sababu gani wamekosa. Maneno haya hayaonyeshi kuwatendea kwa ukatili au kuwaambia maneno makali, bali kuwatendea sawa na hali yao.

78. Je, hawajui kwamba Allah Anayajua mashauriano yao ya siri, na ya kwamba Allah ndiye Ajuaye sana mambo ya ghaibu?

اَلَمْ يَعْلَمُوْٓا اَنَّ اللّٰهَ يَعْلَمُ سِرَّهُمْ وَنَجْوٰىهُمْ وَاَنَّ اللّٰهَ عَلَّامُ الْغُيُوْبِ ﴿٧٨﴾

79. Wale wanaowasingizia kuhusiana na sadaka, waaminio wafanyao wema kwa furaha, na pia wale wasiopata (cha kutoa) ila juhudi yao, basi hao (wasingiziao) wanawafanyia mzaha; Allah Atawalipa mzaha (wao), nao watapata adhabu iumizayo.

اَلَّذِيْنَ يَلْمِزُوْنَ الْمُطَّوِّعِيْنَ مِنَ الْمُؤْمِنِيْنَ فِى الصَّدَقٰتِ وَالَّذِيْنَ لَا يَجِدُوْنَ اِلَّا جُهْدَهُمْ فَيَسْخَرُوْنَ مِنْهُمْ ۙ سَخِرَ اللّٰهُ مِنْهُمْ ۖ وَلَهُمْ عَذَابٌ اَلِيْمٌ ﴿٧٩﴾

80. Uwaombee msamaha au usiwaombee msamaha, hata ukiwaombea msamaha mara sabini, Allah Hatawasamehe. Hayo ni kwa sababu ya kuwa wao wamemkataa Allah na Mtume Wake, na Allah Hawaongozi watu wavunjao amri.

اِسْتَغْفِرْ لَهُمْ اَوْ لَا تَسْتَغْفِرْ لَهُمْ ۚ اِنْ تَسْتَغْفِرْ لَهُمْ سَبْعِيْنَ مَرَّةً فَلَنْ يَّغْفِرَ اللّٰهُ لَهُمْ ۚ ذٰلِكَ بِاَنَّهُمْ كَفَرُوْا بِاللّٰهِ وَرَسُوْلِهٖ ۚ وَاللّٰهُ لَا يَهْدِى الْقَوْمَ الْفٰسِقِيْنَ ﴿٨٠﴾

FUNGU 11

81. Walifurahi walioachwa nyuma kwa sababu ya kukaa nyuma ya Mtume wa Allah na kuchukia kufanya juhudi kwa mali zao na nafsi zao katika njia ya Allah, na wakasema: Msiende (vitani) katika joto. Sema: Moto wa Jahanamu una joto zaidi. Laiti wangefahamu.

فَرِحَ الْمُخَلَّفُوْنَ بِمَقْعَدِهِمْ خِلٰفَ رَسُوْلِ اللّٰهِ وَكَرِهُوْٓا اَنْ يُّجَاهِدُوْا بِاَمْوَالِهِمْ وَاَنْفُسِهِمْ فِىْ سَبِيْلِ اللّٰهِ وَقَالُوْا لَا تَنْفِرُوْا فِى الْحَرِّ ۚ قُلْ نَارُ جَهَنَّمَ اَشَدُّ حَرًّا ۚ لَوْ كَانُوْا يَفْقَهُوْنَ ﴿٨١﴾

82. Basi wacheke kidogo na walie sana, ni malipo ya yale waliyokuwa wakiyachuma.

فَلْيَضْحَكُوْا قَلِيْلًا وَّلْيَبْكُوْا كَثِيْرًا ۚ جَزَآءًۢ بِمَا كَانُوْا يَكْسِبُوْنَ ﴿٨٢﴾

Aya 79. Aya hii inaonyesha ya kuwa wanafiki walitafuta njia ya kuwatiatia ila na kuwalaumu waaminio wa kila namna. Wale waliotoa kwa wingi mali zao na pia wale ambao hawakuwa na cha kutoa. Hapa jambo linalorejewa ni safari ya vita ya kwenda Tabuk. Kabla ya kufunga safari Mtume s.a.w aliwaambia waaminio watoe michango kwa wingi kwa ajili ya safari hii kubwa. Seyidna Uthman alitoa ngamia 300 na dinari 10,000/-, Seyidna Abu Bakar akatoa mali yake yote aliyokuwa nayo. Seyidna Umar akatoa nusu ya mali yake yote. Wanafiki wakaanza kusema ya kuwa wasingetoa hivi ila kwa kutaka kujionyesha tu, na pia wakawasema hivi waaminio wengine waliotoa michango kwa wingi. Upande mwingine waliotoa kidogo wakawacheka.

فَاِنْ رَّجَعَكَ اللّٰهُ اِلٰى طَآئِفَةٍ مِّنْهُمْ فَاسْتَاْذَنُوْكَ لِلْخُرُوْجِ فَقُلْ لَّنْ تَخْرُجُوْا مَعِيَ اَبَدًا وَّلَنْ تُقَاتِلُوْا مَعِيَ عَدُوًّا ؕ اِنَّكُمْ رَضِيْتُمْ بِالْقُعُوْدِ اَوَّلَ مَرَّةٍ فَاقْعُدُوْا مَعَ الْخٰلِفِيْنَ ﴿٨٣﴾

83. Basi Allah Akikurudisha katika taifa moja miongoni mwao na wakikutaka idhini ya kutoka (kwenda vitani), basi sema: Ninyi hamtatoka abadan pamoja nami; wala hamtapigana na maadui pamoja nami. Hakika ninyi mlipenda kukaa mara ya kwanza; basi kaeni pamoja na wabakiao nyuma.

وَلَا تُصَلِّ عَلٰٓى اَحَدٍ مِّنْهُمْ مَّاتَ اَبَدًا وَّلَا تَقُمْ عَلٰى قَبْرِهٖ ؕ اِنَّهُمْ كَفَرُوْا بِاللّٰهِ وَرَسُوْلِهٖ وَمَاتُوْا وَهُمْ فٰسِقُوْنَ ﴿٨٤﴾

84. Wala usimsalie kamwe mmoja wao afapo, wala usisimame kaburini pake. Hakika hao wamemkataa Allah na Mtume Wake, na wakafa hali ni wavunjao amri.

وَلَا تُعْجِبْكَ اَمْوَالُهُمْ وَاَوْلَادُهُمْ ؕ اِنَّمَا يُرِيْدُ اللّٰهُ اَنْ يُّعَذِّبَهُمْ بِهَا فِي الدُّنْيَا وَتَزْهَقَ اَنْفُسُهُمْ وَهُمْ كٰفِرُوْنَ ﴿٨٥﴾

85. Wala zisikuvutie mali zao na watoto wao; Allah Anataka tu kuwaadhibu kwayo katika dunia, na roho zao zitoke hali wao ni makafiri.

وَاِذَآ اُنْزِلَتْ سُوْرَةٌ اَنْ اٰمِنُوْا بِاللّٰهِ وَجَاهِدُوْا مَعَ رَسُوْلِهِ اسْتَاْذَنَكَ اُولُوا الطَّوْلِ مِنْهُمْ وَقَالُوْا ذَرْنَا نَكُنْ مَّعَ الْقٰعِدِيْنَ ﴿٨٦﴾

86. Na inapoteremshwa sura kwamba, Mwaminini Allah na fanyeni juhudi pamoja na Mtume Wake, wenye wasaa miongoni mwao wanakuomba ruhusa, na husema: Tuache tuwe pamoja na wakaao.

رَضُوْا بِاَنْ يَّكُوْنُوْا مَعَ الْخَوَالِفِ وَطُبِعَ عَلٰى قُلُوْبِهِمْ فَهُمْ لَا يَفْقَهُوْنَ ﴿٨٧﴾

87. Waliridhia kuwa pamoja na wabakiao nyuma, na mioyo yao ikapigwa muhuri, kwa hiyo hawafahamu.

لٰكِنِ الرَّسُوْلُ وَالَّذِيْنَ اٰمَنُوْا مَعَهٗ جٰهَدُوْا بِاَمْوَالِهِمْ وَاَنْفُسِهِمْ ؕ وَاُولٰٓئِكَ لَهُمُ الْخَيْرٰتُ ۫ وَاُولٰٓئِكَ هُمُ الْمُفْلِحُوْنَ ﴿٨٨﴾

88. Lakini Mtume pamoja na wale walioamini pamoja naye walifanya jihadi kwa mali zao na nafsi zao; na hao ndio wapatao heri zote; na hao ndio wenye kufaulu.

اَعَدَّ اللّٰهُ لَهُمْ جَنّٰتٍ تَجْرِيْ مِنْ تَحْتِهَا الْاَنْهٰرُ خٰلِدِيْنَ فِيْهَا ؕ ذٰلِكَ الْفَوْزُ الْعَظِيْمُ ﴿٨٩﴾ ع

89. Allah Amewaandalia Bustani zipitazo mito ndani yao, kukaa humo; huo ndio ufaulu mkuu.

Aya 84. Anayekufa katika hali ya ukafiri (akiwa ni kafiri wa wazi au mnafiki aliyehakikishwa), basi hana haki ya kusaliwa na waaminio. Shauri lao liko mikononi mwa Mungu. Anaweza kuwaadhibu au kuwasamehe apendavyo.

FUNGU 12

وَجَآءَ الْمُعَذِّرُوْنَ مِنَ الْاَعْرَابِ لِيُؤْذَنَ لَهُمْ وَقَعَدَ الَّذِيْنَ كَذَبُوا اللّٰهَ وَرَسُوْلَهٗ ؕ سَيُصِيْبُ الَّذِيْنَ كَفَرُوْا مِنْهُمْ عَذَابٌ اَلِيْمٌ ﴿٩٠﴾

90. Na wakaja wenye udhuru miongoni mwa mabedui ili wapewe ruhusa. Na wakakaa (nyuma) wale waliosema uwongo mbele ya Allah na Mtume Wake. Hivi karibuni itawafikia wale waliokufuru miongoni mwao adhabu iumizayo.

لَيْسَ عَلَى الضُّعَفَآءِ وَلَا عَلَى الْمَرْضٰى وَلَا عَلَى الَّذِيْنَ لَا يَجِدُوْنَ مَا يُنْفِقُوْنَ حَرَجٌ اِذَا نَصَحُوْا لِلّٰهِ وَرَسُوْلِهٖ ؕ مَا عَلَى الْمُحْسِنِيْنَ مِنْ سَبِيْلٍ ؕ وَاللّٰهُ غَفُوْرٌ رَّحِيْمٌ ﴿٩١﴾

91. Si kosa juu ya walio dhaifu, wala juu ya wagonjwa, wala juu ya wale wasiopata cha kutoa (kubaki nyuma), wanapokuwa wanyofu kwa Allah na Mtume Wake: hakuna njia ya kuwalaumu wafanyao mema; Na Allah ni Msamehevu, Mrehemevu.

وَّلَا عَلَى الَّذِيْنَ اِذَا مَاۤ اَتَوْكَ لِتَحْمِلَهُمْ قُلْتَ لَاۤ اَجِدُ مَاۤ اَحْمِلُكُمْ عَلَيْهِ ۖ تَوَلَّوْا وَّاَعْيُنُهُمْ تَفِيْضُ مِنَ الدَّمْعِ حَزَنًا اَلَّا يَجِدُوْا مَا يُنْفِقُوْنَ ﴿٩٢﴾

92. Wala (si kosa) juu ya wale waliokufikia ili uwapandishe (juu ya wanyama), ukasema: Sina cha kuwapandisheni juu yake; wakarudi hali macho yao yanachirizisha machozi kwa huzuni ya kukosa kupata cha kutoa.

اِنَّمَا السَّبِيْلُ عَلَى الَّذِيْنَ يَسْتَاْذِنُوْنَكَ وَهُمْ اَغْنِيَآءُ ۚ رَضُوْا بِاَنْ يَّكُوْنُوْا مَعَ الْخَوَالِفِ ۙ وَطَبَعَ اللّٰهُ عَلٰى قُلُوْبِهِمْ فَهُمْ لَا يَعْلَمُوْنَ ﴿٩٣﴾

93. Lawama iko tu kwa wale wanaokuomba ruhusa hali wao ni matajiri; wamependa kuwa pamoja na wabakiao nyuma. Na Allah Amepiga muhuri juu ya mioyo yao, kwa hiyo hawajui.

Aya 90. *Wakaja wenye udhuru,* yaani wanafiki na pia watu wenye imani hafifu ambao hawakuingia katika jeshi lililokwenda Tabuk.

Aya 92. Aya hii inahusu kila wakati. Hapa inaeleza habari za Waislamu saba maskini ambao walitamani sana kwenda katika jihadi, lakini Mtume *s.a.w* alikuwa hana ngamia wa kuwachukua. Hawa watu wakarudi hali macho yao yamejaa machozi. Baadaye Mtume *s.a.w* alipewa ngamia watatu na Seyidna Uthman na wanne wakatolewa na waislamu wengine, basi hao mabwana saba nao wakaingia safarini.

JUZU 11

94. Hivi karibuni watawaleteeni udhuru mtakapo rudi kwao. Sema: Msitoe udhuru hatutawaaminini. Hakika Allah Amekwisha tueleza habari zenu; na karibuni hivi Allah Ataviangalia vitendo vyenu, na Mtume Wake pia. Kisha mtarudishwa kwa Mjuzi wa siri na dhahiri, naye Atawaambieni yale mliyokuwa mkiyatenda.

يَعْتَذِرُوْنَ اِلَيْكُمْ اِذَا رَجَعْتُمْ اِلَيْهِمْ ؕ قُلْ لَّا تَعْتَذِرُوْا لَنْ نُّؤْمِنَ لَكُمْ قَدْ نَبَّاَنَا اللّٰهُ مِنْ اَخْبَارِكُمْ ؕ وَسَيَرَى اللّٰهُ عَمَلَكُمْ وَرَسُوْلُهٗ ثُمَّ تُرَدُّوْنَ اِلٰى عٰلِمِ الْغَيْبِ وَالشَّهَادَةِ فَيُنَبِّئُكُمْ بِمَا كُنْتُمْ تَعْمَلُوْنَ ﴿٩٤﴾

95. Kwa yakini watawaapieni Allah mtakaporudi kwao ili mjitenge nao. Basi jitengeni nao; bila shaka wao ni najisi, na makazi yao ni Jahanamu; ni malipo ya yale waliyokuwa wakiyachuma.

سَيَحْلِفُوْنَ بِاللّٰهِ لَكُمْ اِذَا انْقَلَبْتُمْ اِلَيْهِمْ لِتُعْرِضُوْا عَنْهُمْ ؕ فَاَعْرِضُوْا عَنْهُمْ ؕ اِنَّهُمْ رِجْسٌ ۙ وَّمَاْوٰىهُمْ جَهَنَّمُ ۚ جَزَآءًۢ بِمَا كَانُوْا يَكْسِبُوْنَ ﴿٩٥﴾

96. Wanawaapieni ili muwe radhi nao. Na kama mkiwaridhia, basi hakika Allah Hawi radhi na watu wavunjao amri.

يَحْلِفُوْنَ لَكُمْ لِتَرْضَوْا عَنْهُمْ ۚ فَاِنْ تَرْضَوْا عَنْهُمْ فَاِنَّ اللّٰهَ لَا يَرْضٰى عَنِ الْقَوْمِ الْفٰسِقِيْنَ ﴿٩٦﴾

97. Mabedui wamezidi sana katika kufuru na unafiki, na wameelekea zaidi wasijue mipaka ya yale Aliyoyateremsha Allah juu ya Mtume Wake. Na Allah ni Mjuzi, Mwenye hekima.

اَلْاَعْرَابُ اَشَدُّ كُفْرًا وَّنِفَاقًا وَّاَجْدَرُ اَلَّا يَعْلَمُوْا حُدُوْدَ مَاۤ اَنْزَلَ اللّٰهُ عَلٰى رَسُوْلِهٖ ؕ وَاللّٰهُ عَلِيْمٌ حَكِيْمٌ ﴿٩٧﴾

98. Na miongoni mwa Mabedui wako wale wanaofikiri ya kuwa yale wanayoyatoa katika njia ya Allah ni gharama ya bure na wanawangojeleeni misiba. Na msiba mbaya ni wenye kuwashukia wao tu; na Allah ndiye Asiki-Asikiaye, Ajuaye.

وَمِنَ الْاَعْرَابِ مَنْ يَّتَّخِذُ مَا يُنْفِقُ مَغْرَمًا وَّيَتَرَبَّصُ بِكُمُ الدَّوَآئِرَ ؕ عَلَيْهِمْ دَآئِرَةُ السَّوْءِ ؕ وَاللّٰهُ سَمِيْعٌ عَلِيْمٌ ﴿٩٨﴾

Aya 95. *Ili mjitenge nao,* yaani, ili muwasamehe na msiwaulize sababu. Lakini maneno haya, *basi jitengeni nao,* maana yake msiwe na shauri nao.

وَمِنَ الْاَعْرَابِ مَنْ يُّؤْمِنُ بِاللّٰهِ وَالْيَوْمِ
الْاٰخِرِ وَيَتَّخِذُ مَا يُنْفِقُ قُرُبٰتٍ عِنْدَ اللّٰهِ
وَصَلَوٰتِ الرَّسُوْلِ ؕ اَلَاۤ اِنَّهَا قُرْبَةٌ
لَّهُمْ ؕ سَيُدْخِلُهُمُ اللّٰهُ فِيْ رَحْمَتِهٖ ؕ اِنَّ
اللّٰهَ غَفُوْرٌ رَّحِيْمٌ ﴿۹۹﴾ ع

99. Na wapo katika Mabedui hao wanaomuamini Allah na siku ya Mwisho, na wanayashika yale wanayoyatoa kuwa ni (sababu za) kumkaribia Allah na za kupata dua za Mtume. Sikilizeni! hakika hiyo ni njia ya kupata kwao ukaribu na Allah. Hivi karibuni Allah Atawaingiza katika rehema Yake. Bila shaka Allah ni Msamehevu, Mrehemevu.

FUNGU 13

وَالسّٰبِقُوْنَ الْاَوَّلُوْنَ مِنَ الْمُهٰجِرِيْنَ
وَالْاَنْصَارِ وَالَّذِيْنَ اتَّبَعُوْهُمْ بِاِحْسَانٍ ۙ
رَّضِيَ اللّٰهُ عَنْهُمْ وَرَضُوْا عَنْهُ وَاَعَدَّ
لَهُمْ جَنّٰتٍ تَجْرِيْ تَحْتَهَا الْاَنْهٰرُ خٰلِدِيْنَ
فِيْهَاۤ اَبَدًا ؕ ذٰلِكَ الْفَوْزُ الْعَظِيْمُ ﴿۱۰۰﴾

100. Na waliotangulia mwanzoni miongoni mwa Wahajiri (Wahamiaji) na Ansar (Wasaidizi), na wale waliowafuata kwa hisani, Allah Amewaridhia, nao pia wamemridhia, na Amewaandalia Bustani zipitazo mito ndani yake, watakaa humo milele. Huo ndio ufaulu mkuu.

وَمِمَّنْ حَوْلَكُمْ مِّنَ الْاَعْرَابِ
مُنٰفِقُوْنَ ؕ وَمِنْ اَهْلِ الْمَدِيْنَةِ ۛؔ مَرَدُوْا
عَلَى النِّفَاقِ ۟ لَا تَعْلَمُهُمْ ؕ نَحْنُ
نَعْلَمُهُمْ ؕ سَنُعَذِّبُهُمْ مَّرَّتَيْنِ ثُمَّ
يُرَدُّوْنَ اِلٰى عَذَابٍ عَظِيْمٍ ﴿۱۰۱﴾ ۚ

101. Na katika Mabedui wanaokaa pembezoni mwenu kuna wanafiki, na katika wenyeji wa Madina pia. Wamejikita katika unafiki. Huwajui, Sisi Twawajua. Hivi karibuni Tutawaadhibu mara mbili, kisha watarudishwa kwenye adhabu kubwa.

Aya 99. Qur'an haimnyimi mtu haki yake. Kwa kuwa Waarabu wa Kibedui walisemwa *wamezidi sana katika kufuru na unafiki* (sura 9:97), Aya hii inaonyesha ya kuwa si Mabedui wote waliokuwa hivyo. Pia kati yao walikuwamo watu waaminio sawasawa waliofanya bidii sana kumkaribia Allah.

Aya 100. Masahaba wa Mtume *s.a.w* wanasemwa hapa kuwa wao ni mfano unaostahili kuigwa na watu wengine, kwa kuwa wako mbele katika daraja, na ndio wa kwanza kuamini. Naam, hata wale waliofuata sawasawa katika nyayo za masahaba walikuwa wapenzi wa Mungu. Aya hii inavunja lawama zinazotolewa na watu wa madhehebu nyingine juu ya Makhalifa watatu wa kwanza wa Mtume *s.a.w* na juu ya masahaba wake wengine wakubwa wakubwa.

وَاٰخَرُوْنَ اعْتَرَفُوْا بِذُنُوْبِهِمْ خَلَطُوْا عَمَلًا صَالِحًا وَّاٰخَرَ سَيِّئًا ؕ عَسَى اللّٰهُ اَنْ يَّتُوْبَ عَلَيْهِمْ ؕ اِنَّ اللّٰهَ غَفُوْرٌ رَّحِيْمٌ ﴿۱۰۲﴾

102. Na wako wengine waliokiri dhambi zao; wakachanganya vitendo vizuri na vingine vibaya. Huenda Allah Akapokea toba zao. Hakika Allah ni Msamehevu, Mrehemevu.

خُذْ مِنْ اَمْوَالِهِمْ صَدَقَةً تُطَهِّرُهُمْ وَتُزَكِّيْهِمْ بِهَا وَصَلِّ عَلَيْهِمْ ؕ اِنَّ صَلٰوتَكَ سَكَنٌ لَّهُمْ ؕ وَاللّٰهُ سَمِيْعٌ عَلِيْمٌ ﴿۱۰۳﴾

103. Chukua sadaka katika mali zao, ambayo kwayo utawasafisha na kuwatakasa, na uwaombee. Hakika dua zako ni zenye kuwapatia utulivu; na Allah ndiye Asikiaye, Ajuaye.

اَلَمْ يَعْلَمُوْٓا اَنَّ اللّٰهَ هُوَ يَقْبَلُ التَّوْبَةَ عَنْ عِبَادِهٖ وَيَاْخُذُ الصَّدَقٰتِ وَاَنَّ اللّٰهَ هُوَ التَّوَّابُ الرَّحِيْمُ ﴿۱۰۴﴾

104. Je, hawajui ya kwamba Allah ndiye Anayepokea toba ya watumishi Wake na kuzipokea sadaka, na ya kwamba Allah ni Mwenye kupokea toba, Mwenye rehema?

وَقُلِ اعْمَلُوْا فَسَيَرَى اللّٰهُ عَمَلَكُمْ وَرَسُوْلُهٗ وَالْمُؤْمِنُوْنَ ؕ وَسَتُرَدُّوْنَ اِلٰى عٰلِمِ الْغَيْبِ وَالشَّهَادَةِ فَيُنَبِّئُكُمْ بِمَا كُنْتُمْ تَعْمَلُوْنَ ﴿۱۰۵﴾

105. Na sema: Tendeni, hivi karibuni Allah Ataziona amali zenu, na Mtume Wake na waaminio pia. Na kwa yakini mtarudishwa kwa Mjuzi wa siri na dhahiri; naye Atawaambieni mliyokuwa mkiyatenda.

وَاٰخَرُوْنَ مُرْجَوْنَ لِاَمْرِ اللّٰهِ اِمَّا يُعَذِّبُهُمْ وَاِمَّا يَتُوْبُ عَلَيْهِمْ ؕ وَاللّٰهُ عَلِيْمٌ حَكِيْمٌ ﴿۱۰۶﴾

106. Na wako wengine ambao wamewekwa katika mkao wa kuingojea amri ya Allah. Anaweza kuamua Awaadhibu au Awaelekee kwa rehema. Na Allah ni Mjuzi Mwenye hekima.

وَالَّذِيْنَ اتَّخَذُوْا مَسْجِدًا ضِرَارًا وَّكُفْرًا

107. Na wale ambao wamejenga msikiti ili kuleta madhara na kueneza ukafiri

Aya 105. Ingawa baadhi ya Waislamu waliotajwa katika Aya 104 walitubu, na toba yao ikakubaliwa, lakini hapa wanaambiwa ya kuwa toba haiwezi kuwa kamili mpaka mtu ameonyesha baadaye kwa matendo yake ya kuwa kweli amejisahihisha. Hivyo watu hawa wanaonywa katika Aya hii ya kuwa matendo yao ya baadaye yataangaliwa sana.

Aya 107. Aya hii inaeleza habari za hila iliyofanywa na mtu mmoja aitwaye Abu 'Aamir

وَّتَفْرِيْقًۢا بَيْنَ الْمُؤْمِنِيْنَ وَ اِرْصَادًا لِّمَنْ حَارَبَ اللّٰهَ وَ رَسُوْلَهٗ مِنْ قَبْلُ ؕ وَلَيَحْلِفُنَّ اِنْ اَرَدْنَاۤ اِلَّا الْحُسْنٰى ؕ وَاللّٰهُ يَشْهَدُ اِنَّهُمْ لَكٰذِبُوْنَ ﴿۱۰۷﴾

na kusababisha utengano miongoni mwa waaminio, na kuufanya kuwa mahali pa kumhifadhi yule ambaye tayari amekwisha tangaza vita dhidi ya Allah na Mtume wake, bila shaka wataapa: Hatukukusudia ila wema. Lakini Allah Anashuhudia kwa hakika wao ni waongo.

لَا تَقُمْ فِيْهِ اَبَدًا ؕ لَمَسْجِدٌ اُسِّسَ عَلَى التَّقْوٰى مِنْ اَوَّلِ يَوْمٍ اَحَقُّ اَنْ تَقُوْمَ فِيْهِ ؕ فِيْهِ رِجَالٌ يُّحِبُّوْنَ اَنْ يَّتَطَهَّرُوْا ؕ وَاللّٰهُ يُحِبُّ الْمُطَّهِّرِيْنَ ﴿۱۰۸﴾

108. Usisimame humo kabisa. Hakika msikiti uliojengwa juu ya msingi wa utawa tangu siku ya kwanza unastahili zaidi wewe usimame humo. Humo wamo watu wanaopenda kujitakasa. Na Allah Anawapenda wajitakasao.

اَفَمَنْ اَسَّسَ بُنْيَانَهٗ عَلٰى تَقْوٰى مِنَ اللّٰهِ وَ رِضْوَانٍ خَيْرٌ اَمْ مَّنْ اَسَّسَ بُنْيَانَهٗ عَلٰى شَفَا جُرُفٍ هَارٍ فَانْهَارَ بِهٖ فِيْ نَارِ جَهَنَّمَ ؕ وَاللّٰهُ لَا يَهْدِي الْقَوْمَ الظّٰلِمِيْنَ ﴿۱۰۹﴾

109. Je, aliyeweka msingi wa jengo lake juu ya utawa wa Allah na radhi (Yake), ni mbora au aliyeweka msingi wa jengo lake juu ya ukingo wa shimo unaopukutika udongo wake, ukaanguka pamoja naye katika moto wa Jahanamu? Na Allah hawaongozi watu wadhalimu.

---

wa kabila la Khazraj wa Madina, ambaye alikuwa adui mkubwa wa Uislamu. Baada ya vita vya Badri Abu 'Aamir alikimbilia Makka, na huko akawachochea watu wa Makka walipe kisasi. Katika vita vya Uhud huyu Abu 'Aamir alikuwa katika jeshi la watu wa Makka. Alipojua kuwa kuna wanafiki Madina akaanza kuarifiana nao kwa nia ya kuuchimba Uislamu. Rafiki zake ndio waliojenga msikiti mahali paitwapo Kuba, kitongoji cha Madina, ili kuendeshea humo habari za siri za kueneza uwongo juu ya dini ya Kiislamu. Jengo lao lilimalizika Mtume s.a.w alipokuwa karibu kuondoka kwenda Tabuk. Wakamwomba Mtume *s.a.w* aubarikie msikiti huo kwa kusalia humo. Mtume, hali hajui nia zao mbaya, alikubali na akaahidi kuwatendea walivyomwomba atakaporudi kutoka safari. Katika muda huu Aya hii ikateremka, na alipokuwa akirudi Madina akaamrisha msikiti ule utiwe moto na uvunjwe kabisa (Muhit). Msikiti huo unaitwa *Masjid Dhiraar,* yaani msikiti wa udhia.

Aya 108. *Msikiti uliojengwa juu ya msingi wa utawa tangu siku ya kwanza* ni msikiti wa Kuba uliojengwa mahali aliposhuka Mtume *s.a.w* kabla kuingia Madina, siku aliyofika pale kutoka Makka. Lakini kuna wengine wasemao, maneno hayo yanahusu msikiti aliojenga Mtume Madina unaoitwa *Masjid-un-Nabii* (Msikiti wa Nabii). Mpango wa maneno ya Aya hii unaonekana kupendelea wasemao msikiti huo ni ule wa Madina.

لَا يَزَالُ بُنْيَانُهُمُ الَّذِىْ بَنَوْا رِيْبَةً فِىْ قُلُوْبِهِمْ اِلَّاۤ اَنْ تَقَطَّعَ قُلُوْبُهُمْ ؕ وَاللّٰهُ عَلِيْمٌ حَكِيْمٌ ﴿۱۱۰﴾ ع

110. Jengo walilolijenga daima litakuwa sababu ya kutia wasiwasi mioyoni mwao, isipokuwa mioyo yao ikatike vipande vipande (kutokana na hofu ya Allah). Na Allah ni Mjuzi, Mwenye hekima.

FUNGU 14

اِنَّ اللّٰهَ اشْتَرٰى مِنَ الْمُؤْمِنِيْنَ اَنْفُسَهُمْ وَاَمْوَالَهُمْ بِاَنَّ لَهُمُ الْجَنَّةَ ؕ يُقَاتِلُوْنَ فِىْ سَبِيْلِ اللّٰهِ فَيَقْتُلُوْنَ وَيُقْتَلُوْنَ ۟ وَعْدًا عَلَيْهِ حَقًّا فِى التَّوْرٰىةِ وَالْاِنْجِيْلِ وَالْقُرْاٰنِ ؕ وَمَنْ اَوْفٰى بِعَهْدِهٖ مِنَ اللّٰهِ فَاسْتَبْشِرُوْا بِبَيْعِكُمُ الَّذِىْ بَايَعْتُمْ بِهٖ ؕ وَذٰلِكَ هُوَ الْفَوْزُ الْعَظِيْمُ ﴿۱۱۱﴾

111. Hakika Allah Amenunua kwa waaminio nafsi zao na mali zao ili wapate Pepo. Wanapigana katika njia ya Allah, kwa hiyo wanaua na wanauawa. Hii ndio ahadi iliyolazimu juu Yake katika Taurati na Injili na Qur'an. Na ni nani aitekelezaye zaidi ahadi yake kuliko Allah? Basi furahini kwa biashara yenu mliyofanya naye. Na huo ndio ufaulu mkuu.

اَلتَّآئِبُوْنَ الْعٰبِدُوْنَ الْحٰمِدُوْنَ السَّآئِحُوْنَ الرّٰكِعُوْنَ السّٰجِدُوْنَ الْاٰمِرُوْنَ بِالْمَعْرُوْفِ وَالنَّاهُوْنَ عَنِ الْمُنْكَرِ وَالْحٰفِظُوْنَ لِحُدُوْدِ اللّٰهِ ؕ وَبَشِّرِ الْمُؤْمِنِيْنَ ﴿۱۱۲﴾

112. (Hao ndio) wanaotubu, wanaoabudu, wanaotukuza, wanaofunga saumu, wanaorukuu, wanaosujudu, wanaoamuru yaliyo mema, na wanaozuia yaliyo mabaya, na wanaohifadhi mipaka ya Allah - na wape habari njema waaminio.

مَا كَانَ لِلنَّبِىِّ وَالَّذِيْنَ اٰمَنُوْۤا اَنْ يَّسْتَغْفِرُوْا لِلْمُشْرِكِيْنَ وَلَوْ كَانُوْۤا اُولِىْ قُرْبٰى مِنْۢ بَعْدِ مَا تَبَيَّنَ لَهُمْ اَنَّهُمْ اَصْحٰبُ الْجَحِيْمِ ﴿۱۱۳﴾

113. Haimpasi Nabii na wale walioamini kuwaombea ghofira washirikina, ijapokuwa ni jamaa wa karibu, baada ya kuwabainikia kuwa wao ni watu wa Motoni.

وَمَا كَانَ اسْتِغْفَارُ اِبْرٰهِيْمَ لِاَبِيْهِ اِلَّا عَنْ مَّوْعِدَةٍ وَّعَدَهَاۤ اِيَّاهُ ۚ فَلَمَّا تَبَيَّنَ لَهٗۤ اَنَّهٗ عَدُوٌّ لِّلّٰهِ تَبَرَّاَ مِنْهُ ؕ اِنَّ اِبْرٰهِيْمَ

114. Wala haikuwa kwa Ibrahimu kumuombea ghofira baba yake ila kwa sababu ya ahadi aliyokwishafanya naye, lakini ilipombainikia kwamba yeye ni adui wa Allah, alijiepusha naye.

Aya 112. Aya hii inaendeleza Aya 111, na inaonyesha kuwa wanaosemwa hapa ni Masahaba wa Mtume *s.a.w.* na wale wanaowafuata sawasawa.

Kwa yakini Ibrahimu alikuwa mpole wa moyo, mvumilivu.

لَاَوَّاهٌ حَلِيْمٌ ﴿١١٤﴾

115. Na haimpasi Allah kuwapoteza watu baada ya kuwa Amewaongoza: hata Awabainishie watakayojiepusha nayo. Hakika Allah Anajua kila kitu.

وَمَا كَانَ اللّٰهُ لِيُضِلَّ قَوْمًا بَعْدَ اِذْ هَدٰىهُمْ حَتّٰى يُبَيِّنَ لَهُمْ مَّا يَتَّقُوْنَ ؕ اِنَّ اللّٰهَ بِكُلِّ شَيْءٍ عَلِيْمٌ ﴿١١٥﴾

116. Hakika Allah Anao ufalme wa mbingu na ardhi; Huhuisha na Hufisha; nanyi hamna mlinzi wala msaidizi minghairi ya Allah.

اِنَّ اللّٰهَ لَهٗ مُلْكُ السَّمٰوٰتِ وَالْاَرْضِ ؕ يُحْيٖ وَيُمِيْتُ ؕ وَمَا لَكُمْ مِّنْ دُوْنِ اللّٰهِ مِنْ وَّلِيٍّ وَّلَا نَصِيْرٍ ﴿١١٦﴾

117. Bila shaka Allah Amemwelekea Mtume na Wahajiri (wahamiaji) na Waanswar (Wasaidizi) waliomfuata yeye katika saa ya dhiki, baada ya kukaribia kugeuka mioyo ya baadhi yao, kisha Akawaelekea. Kwa yakini Yeye kwao ni Mpole, Mrehemevu.

لَقَدْ تَّابَ اللّٰهُ عَلَى النَّبِيِّ وَالْمُهٰجِرِيْنَ وَالْاَنْصَارِ الَّذِيْنَ اتَّبَعُوْهُ فِيْ سَاعَةِ الْعُسْرَةِ مِنْۢ بَعْدِ مَا كَادَ يَزِيْغُ قُلُوْبُ فَرِيْقٍ مِّنْهُمْ ثُمَّ تَابَ عَلَيْهِمْ ؕ اِنَّهٗ بِهِمْ رَءُوْفٌ رَّحِيْمٌ ﴿١١٧﴾

118. Na (pia Akawaelekea) wale watatu walioachwa nyuma, hata ardhi ikawa finyu juu yao licha ya wasaa wake, na nafsi zao zikadhikika, na wakadhani ya kwamba hapana pa kumkimbia Allah isipokuwa (kuelekea) Kwake; kisha Akawaelekea ili wapate kutubu. Hakika Allah ndiye Apokeaye toba, Mrehemevu.

وَّعَلَى الثَّلٰثَةِ الَّذِيْنَ خُلِّفُوْا ؕ حَتّٰۤى اِذَا ضَاقَتْ عَلَيْهِمُ الْاَرْضُ بِمَا رَحُبَتْ وَضَاقَتْ عَلَيْهِمْ اَنْفُسُهُمْ وَظَنُّوْۤا اَنْ لَّا مَلْجَاَ مِنَ اللّٰهِ اِلَّاۤ اِلَيْهِ ؕ ثُمَّ تَابَ عَلَيْهِمْ لِيَتُوْبُوْا ؕ اِنَّ اللّٰهَ هُوَ التَّوَّابُ الرَّحِيْمُ ﴿١١٨﴾ ع

Aya 117. Neno *Amemwelekea* si lazima liwe na maana ya kupokea toba. Hapa lina maana ya "kumfadhili mtu," maana hapa limetumiwa kwa ajili ya Mtume s.a.w na kwa ajili ya waliomfuata kwa furaha katika saa ile ya dhiki. Huu ulikuwa ni wakati kwa Mtume *s.a.w.* na wafuasi wake kupata thawabu, siyo kusamehewa.

Aya 118. Aya hii inaeleza habari za Ka'b bin Maalik, Hilaal bin Umayya na Muraar bin Rabii'a, ambao habari zao zimetangulia kutajwa katika sura 9:106. Hawa walikuwa Waislamu wema, lakini wakakosa kuingia katika safari ya vita vya Tabuk; basi Mtume aliporudi Madina, akaamrisha watu wasiwe na jambo lo lote nao, hata wasiseme nao. Marufuku hii iliendelea kwa siku zisizo chache kuliko hamsini. Walipotubu kwa uaminifu na wakakubali kuchukua taabu hii kwa nia safi walisamehewa kama inavyoonyeshwa katika Aya hii.

FUNGU 15

119. Enyi mlioamini, Mcheni Allah na kuweni pamoja na wasemao kweli.

يٰٓاَيُّهَا الَّذِيْنَ اٰمَنُوا اتَّقُوا اللّٰهَ وَكُوْنُوْا مَعَ الصّٰدِقِيْنَ ﴿١١٩﴾

120. Haikuwapasa watu wa Madina na Mabedui wakaao pembeni mwao kubaki nyuma ya Mtume wa Allah wala kujipendelea nafsi zao kuliko nafsi yake. Hayo ni kwa sababu ya kuwa haiwafikii kiu wala taabu wala njaa katika njia ya Allah,wala hawaikanyagi njia iwachukizayo makafiri, Wala hawapati chochote kutoka kwa maadui ila badala yake wanaandikiwa kitendo chema. Hakika Allah Hapotezi ujira wa watendao wema.

مَا كَانَ لِاَهْلِ الْمَدِيْنَةِ وَمَنْ حَوْلَهُمْ مِّنَ الْاَعْرَابِ اَنْ يَّتَخَلَّفُوْا عَنْ رَّسُوْلِ اللّٰهِ وَلَا يَرْغَبُوْا بِاَنْفُسِهِمْ عَنْ نَّفْسِهٖ ؕ ذٰلِكَ بِاَنَّهُمْ لَا يُصِيْبُهُمْ ظَمَاٌ وَّلَا نَصَبٌ وَّلَا مَخْمَصَةٌ فِيْ سَبِيْلِ اللّٰهِ وَلَا يَطَـُٔوْنَ مَوْطِئًا يَّغِيْظُ الْكُفَّارَ وَلَا يَنَالُوْنَ مِنْ عَدُوٍّ نَّيْلًا اِلَّا كُتِبَ لَهُمْ بِهٖ عَمَلٌ صَالِحٌ ؕ اِنَّ اللّٰهَ لَا يُضِيْعُ اَجْرَ الْمُحْسِنِيْنَ ﴿١٢٠﴾

121. Wala hawatoi kinachotolewa, kidogo wala kikubwa, wala hawalivuki bonde ila wanaandikiwa ya kwamba Allah Awalipe mema ya yale waliyokuwa wakiyatenda.

وَلَا يُنْفِقُوْنَ نَفَقَةً صَغِيْرَةً وَّلَا كَبِيْرَةً وَّلَا يَقْطَعُوْنَ وَادِيًا اِلَّا كُتِبَ لَهُمْ لِيَجْزِيَهُمُ اللّٰهُ اَحْسَنَ مَا كَانُوْا يَعْمَلُوْنَ ﴿١٢١﴾

122. Wala haiwezekani kwa waaminio kutoka wote. Lakini mbona halitoki kundi katika kila taifa miongoni mwao kujielimisha vema dini na kuwaonya watu wao watakapowarudia, ili wapate kujihadhari?

وَمَا كَانَ الْمُؤْمِنُوْنَ لِيَنْفِرُوْا كَآفَّةً ؕ فَلَوْلَا نَفَرَ مِنْ كُلِّ فِرْقَةٍ مِّنْهُمْ طَآئِفَةٌ لِّيَتَفَقَّهُوْا فِي الدِّيْنِ وَلِيُنْذِرُوْا قَوْمَهُمْ اِذَا رَجَعُوْٓا اِلَيْهِمْ لَعَلَّهُمْ يَحْذَرُوْنَ ﴿١٢٢﴾

FUNGU 16

123. Enyi mlioamini, piganeni na wale walio karibu yenu katika makafiri na waukute ugumu kwenu; na jueni ya kwamba Mwenyezi MunguYu pamoja na wamwogopao.

يٰٓاَيُّهَا الَّذِيْنَ اٰمَنُوْا قَاتِلُوا الَّذِيْنَ يَلُوْنَكُمْ مِّنَ الْكُفَّارِ وَلْيَجِدُوْا فِيْكُمْ غِلْظَةً ؕ وَاعْلَمُوْٓا اَنَّ اللّٰهَ مَعَ الْمُتَّقِيْنَ ﴿١٢٣﴾

124. Na inapoteremshwa sura yoyote, basi wako miongoni mwao wasemao: Ni nani miongoni mwenu hii inawazidishia imani? Basi ama wale walioamini inawazidishia imani, nao wanafurahi.

وَاِذَا مَآ اُنْزِلَتْ سُوْرَةٌ فَمِنْهُمْ مَّنْ يَّقُوْلُ اَيُّكُمْ زَادَتْهُ هٰذِهٖٓ اِيْمَانًا ۚ فَاَمَّا الَّذِيْنَ اٰمَنُوْا فَزَادَتْهُمْ اِيْمَانًا وَّهُمْ يَسْتَبْشِرُوْنَ ﴿١٢٤﴾

وَاَمَّا الَّذِيْنَ فِيْ قُلُوْبِهِمْ مَّرَضٌ فَزَادَتْهُمْ رِجْسًا اِلٰى رِجْسِهِمْ وَمَاتُوْا وَهُمْ كٰفِرُوْنَ ﴿١٢٥﴾

125. Waama wale wenye ugonjwa mioyoni mwao, basi inawazidishia uchafu juu ya uchafu wao, nao wanakufa hali makafiri.

اَوَلَا يَرَوْنَ اَنَّهُمْ يُفْتَنُوْنَ فِيْ كُلِّ عَامٍ مَّرَّةً اَوْ مَرَّتَيْنِ ثُمَّ لَا يَتُوْبُوْنَ وَلَا هُمْ يَذَّكَّرُوْنَ ﴿١٢٦﴾

126. Je, hawaoni ya kwamba wanajaribiwa kila mwaka mara moja au mara mbili? Kisha hawatubu wala hawashiki nasaha.

وَاِذَا مَاۤ اُنْزِلَتْ سُوْرَةٌ نَّظَرَ بَعْضُهُمْ اِلٰى بَعْضٍ ؕ هَلْ يَرٰىكُمْ مِّنْ اَحَدٍ ثُمَّ انْصَرَفُوْا ؕ صَرَفَ اللّٰهُ قُلُوْبَهُمْ بِاَنَّهُمْ قَوْمٌ لَّا يَفْقَهُوْنَ ﴿١٢٧﴾

127. Na inapoteremshwa sura yoyote, hutazamana wao kwa wao, (kana kwamba wanasema kwa ishara): Je, yuko ye yote anayewaona? Kisha hugeuka na kuondoka. Allah Ameigeuza mioyo yao kwa kuwa wao ni watu wasiofahamu.

لَقَدْ جَآءَكُمْ رَسُوْلٌ مِّنْ اَنْفُسِكُمْ عَزِيْزٌ عَلَيْهِ مَا عَنِتُّمْ حَرِيْصٌ عَلَيْكُمْ بِالْمُؤْمِنِيْنَ رَءُوْفٌ رَّحِيْمٌ ﴿١٢٨﴾

128. Bila shaka amewafikieni Mtume kutoka miongoni mwenu; yanamhuzunisha yanayowataabisheni, anawahangaikieni (ili mpate heri), kwa waaminio ni mpole, mrehemevu.

فَاِنْ تَوَلَّوْا فَقُلْ حَسْبِيَ اللّٰهُ ۖ لَاۤ اِلٰهَ اِلَّا هُوَ ؕ عَلَيْهِ تَوَكَّلْتُ وَ هُوَ رَبُّ الْعَرْشِ الْعَظِيْمِ ﴿١٢٩﴾ ع

129. Lakini kama wakikengeuka, basi sema: Allah ndiye Anitoshaye, hakuna aabudiwaye ila Yeye tu; nategemea Kwake; naye ndiye Mola wa Arshi kuu.

Aya 128. Japo Aya hii ni fupi tu lakini imeeleza sifa tano kubwa za Mtume Muhammad *s.a.w.* Kwanza, Mungu anasema yeye ni Mtume. Pili, yeye ni Mtume aliyetolewa miongoni mwetu. Tatu, ni mtu ambaye havumilii kuona wengine wanapata taabu. Nne, ni mtu mwenye shauku sana ya kwamba watu wawe katika hali njema, na tano ya kwamba yeye ni mtu mwenye huruma sana kwa watu waliopokea mafundisho yake.

Aya 129. Aya hii ambayo ni ya mwisho katika sura hii inawajulisha wasioamini ya kuwa Mtume *s.a.w.* kuwaita kwenye haki ni faida yao wenyewe; na kama wakikataa, basi yeye hatapata dhara yo yote.

سُوْرَةُ يُوْنُسَ مَكِّيَّةٌ وَّ هِيَ مَعَ الْبَسْمَلَةِ مِائَةٌ وَّ عَشْرُ اٰيَاتٍ وَّ اَحَدَ عَشَرَ رُكُوْعًا

10. SURA YUUNUS

Imeteremshwa Makka

Ina mafungu 11 na Aya 110 pamoja na Bismillahi

بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ ①

الٓرٰ ۚ تِلْكَ اٰيٰتُ الْكِتٰبِ الْحَكِيْمِ ② ع

اَكَانَ لِلنَّاسِ عَجَبًا اَنْ اَوْحَيْنَآ اِلٰى رَجُلٍ
مِّنْهُمْ اَنْ اَنْذِرِ النَّاسَ وَبَشِّرِ الَّذِيْنَ اٰمَنُوْٓا
اَنَّ لَهُمْ قَدَمَ صِدْقٍ عِنْدَ رَبِّهِمْ ؕ قَالَ ع
الْكٰفِرُوْنَ اِنَّ هٰذَا لَسٰحِرٌ مُّبِيْنٌ ③

1. Kwa jina la Allah, Mwingi wa rehema, Mwingi wa ukarimu.

2. Mimi ndiye Allah Nionaye. Hizi ni Aya za Kitabu chenye hekima.

3. Je, ni ajabu kwa watu ya kwamba Tumemfunulia mtu miongoni mwao kuwa: uwaonye watu na uwape walio-amini habari njema ya kwamba hatua yao mbele ya Mola wao ni ya ukweli. Makafiri wakasema: Hakika huyu ni mchawi dhahiri.

Sura hii ilishuka Makka. Baadhi ya wafasiri wanaeleza ya kwamba Aya zake nyingine zilishuka Madina; lakini rai yao haina hakika. Sura hii imeitwa Yuunus kwa sababu habari inayoelezwa ndani yake inategemea tukio maalumu lililotokea wakati wa Nabii Yunus. Sura nyingi za Qur'an zimepewa majina ya Mitume au ya vitu fulani, si ovyo, bali kuonyesha ya kuwa habari zake zina ufungamano na watu hao au vitu hivyo.

Aya 2. *Alif Laam Raa.* Maneno haya ni kifupisho cha *Anallaahu Araa* (Mimi ndiye Allah, Nionaye). Habari zaidi za *Muqatta'aat* (vifupisho) tazama chini ya sura 2:2.

Alhakiim (Chenye hekima). Neno hili pia linaonyesha sifa tatu mbalimbali za Qur'an: (a) Ya kwamba imejaa busara, ina msingi wa elimu zote za dini na inafundisha kweli tupu; (b) ina mafundisho yanayofaa katika nyakati zote na katika hali zote: (c) inatoa hukumu ya haki katika hitilafu zote za dini.

Aya 3. Inasadikiwa ya kuwa Aya hii ilishuka wakati makafiri waliposema kwa kebehi, "Je, Mungu hakupata mtu mwingine wa kumtuma kuwa Mtume Wake isipokuwa huyu yatima wa Abu Taalib?" Hivi ndivyo makafiri walivyomdharau Mtume *s.a.w.* hata hawakutaka kutaja jina la baba yake na wakasema ni mtoto wa mtu asiye na jina, ambaye amelelewa na mtu mwingine,

4. Bila shaka Mola wenu ni Allah Ambaye Aliziumba mbingu na ardhi katika nyakati sita, kisha Akastawi juu ya Arshi. Hutengeneza (kila) jambo. Hakuna mwombezi ila baada ya idhini Yake. Huyu ndiye Allah, Mola wenu. Basi Mwabuduni Yeye. Je, hamshiki nasaha?

اِنَّ رَبَّكُمُ اللّٰهُ الَّذِیْ خَلَقَ السَّمٰوٰتِ
وَالْاَرْضَ فِیْ سِتَّةِ اَیَّامٍ ثُمَّ اسْتَوٰی
عَلَی الْعَرْشِ ؕ یُدَبِّرُ الْاَمْرَ ؕ مَا مِنْ شَفِیْعٍ
اِلَّا مِنْۢ بَعْدِ اِذْنِهٖ ؕ ذٰلِكُمُ اللّٰهُ رَبُّكُمْ
فَاعْبُدُوْهُ ؕ اَفَلَا تَذَكَّرُوْنَ ۝۳

Aya 4. Katika Aya hii, neno *Ayyaam* (Nyakati), ambalo umoja wake ni *Yaum,* halihusu siku ya saa ishirini na nne inayopambanuka kwa kucha na kuchwa jua, kwa sababu iliyo wazi ya kwamba Aya yenyewe inaeleza habari za wakati uliokuwako hata kabla jua halijaumbwa. Neno hilo hapa linatumika kwa maana ya wakati tu (tazama sura 1:4).

Wanazuoni wakubwa wengi kama Mujahid, Ahmad bin Hambal na Ibni Abbas wana maoni ya kwamba, hapa neno *yaum* mradi wake ni miaka elfu (Kathir na Ma'aani, maelezo ya sura 7:55). Wamechukua fikra hii katika sura 22:48 inayosema kwamba kuna siku iliyo sawa na miaka elfu.

Kwa hakika wako sawa kabisa kwa kushika ya kwamba neno *yaum* katika Aya hii halionyeshi siku ya mzunguko wa ardhi; lakini hawako sawa kwa kushika ya kwamba siku hii ni ya miaka elfu, maana Qur'an pia inasema ya kwamba kuna siku iliyo sawa na miaka elfu hamsini (sura 70:5).

Kama tutahesabu siku 6 za kipimo hiki cha miaka 50,000 kwa siku, itaonyesha ya kwamba kuumbwa mbingu na ardhi kulikamilika katika muda wa miaka 300,000 (mia tatu elfu). Lakini hatuwezi kusema ya kwamba Allah ametubainishia kipimo cha siku Zake zote. Ikiwa baadhi ya siku za Mungu zina urefu wa miaka elfu moja, na siku Zake nyingine zina urefu wa miaka hamsini elfu, inawezekana kuwe na siku Zake nyingine zenye urefu wa miaka lukuki.

Elimu ya *sayansi* imevumbua ya kwamba mbingu na nchi kufikia hali viliyo nayo leo ilichukua miaka mamilioni. Njozi ya mwanachuoni mkuu wa Kiislamu, Muhyi-d-Din Ibni Arabi, pia inatuelekeza kwenye jambo hili hili (tazama sura 2:31).

Hivyo, kweli ni hii ya kwamba hatuwezi kukata shauri, hizi "siku sita" zina uerfu wa miaka mingapi uliochukua kuumbika mbingu na ardhi. Tunayoweza kusema ni kwamba Allah huleta mabadiliko mbalimbali, baadhi ya nyakati zikiwa na urefu wa miaka elfu, nyingine miaka elfu hamsini, na bado nyingine zenye miaka zaidi ya hiyo, na zote hizo kutiwa pamoja kuumbwa mbingu na ardhi kukatimia nyakati sita. Pia tazama sura 7:55.

Daima itaonekana ya kwamba upinzani unapoletwa juu ya Aya mojawapo ya Qur'an, Aya au fungu linalofuata linatoa majibu ya upinzani huo. Mara nyingi swali au hoja yenyewe inayoletwa haitajwi bali jawabu tu linatolewa.

Majibu haya yanakuwa ni kiungo kinachounganisha mambo yanayopita katika fikira za msomaji na maelezo ya Qur'an yenyewe. Hivyo, msomaji anakuta ya kwamba mara tu swali linapozuka moyoni mwake, anapata jibu papo kwa papo.

Hao ambao hawana habari na maarifa haya ya Qur'an ya kimoyo wanaelekea kudhani ya kwamba hakuna mpango maalumu katika Aya za Qur'an, ilhali kosa lote ni lao wenyewe, maana hawajali kuzizamia Aya za Qur'an kwa kuzifikiria.

Aya hii tunayoieleza inajibu swali linalotokana na Aya iliyotangulia. Swali lenyewe ni hili; inawezekanaje Waislamu kustawi na kufanikiwa hali hakuna alama zilizo bayana zinazoonyesha kuwa watafanikiwa? Kwa hakika Aya iliyotangulia iliwaahidi Waislamu kufanikiwa wakati ambao hawakuwa salama hata katika nyumba zao wenyewe, wakizungukwa na maadui jabari kila upande.

kama desturi, wakafikiri ya kwamba ahadi zile za kufanikiwa Waislamu baadaye zilikuwa ni kutazamia yasiyowezekana.

Ubishi huu unaozuka moyoni umejibiwa na Aya hii, inayoeleza ya kwamba alama za mafanikio ya baadaye hazina haja zionekane mara moja, na ya kwamba katika jambo hili mpango wa mambo ya kiakhera unafanana na mpango wa mambo ya kidunia. Hivyo msomaji anavutwa kuangalia ya kwamba mbingu na ardhi viliumbwa katika nyakati sita, na kuonyesha ya kwamba kama ililazimika bishara za neno la Mungu zitimie hivihivi, basi mbingu na ardhi pia zingezuka vu - mara moja. Lakini kuumbwa kwao kulichukua mizunguko sita mirefu mirefu hata vikakamilika kuwa kama hivi vilivyo. Hivyo, kama mbingu na ardhi vimeumbwa pasipo cho chote kwa miaka mamilioni havikadhibishi kuumbwa kwao na Allah, inawezekanaje kufanyiwa shaka mafanikio ya Mtume *s.a.w.* kwa sababu ya kwamba alama za kufanikiwa huko hazionekani, au kufanyiwa shaka ya kwamba ujumbe wake hauwezi kutoka kwa Allah? Kazi za Allah hufanyika kwa mipango maalumu iliyopangika vizuri, na mara nyingi huwa mipango hiyo haionekani na macho ya watu.

Neno *'Arshi* (Arshi au kiti cha Enzi) linahitaji kuelezwa. Kwa kuzifikiria kwa uangalifu sana Aya zote zenye neno *'Arshi,* inabainika ya kwamba neno hili linaonyesha sifa zilizo bora za Allah. Yaani sifa hizo zisizopatikana katika kiumbe cho chote ambazo zinaitwa *Sifaat tanziihiyyah.* Sifa hizi ni za milele na hazibadiliki, nazo zinadhihirishwa na sifa nyingine za Allah zinazoitwa *Sifaat tashbiihiyyah,* yaani sifa zinazopatikana kwa wingi au kwa uchache katika viumbe Vyake pia. *Sifaat tanziihiyyah* ndizo zinazosemwa kuwa zinaibeba Arshi.

Katika sura 69:18, tunasoma kwamba (sifa) nane zitabeba kiti cha Enzi cha Allah siku hiyo. Hesabu ya "nane" katika Aya hii inahusu sifa nane atakazojionyeshea Allah siku ya Kiyama, kama vile anavyojionyesha kwa sifa Zake nne (zinazotajwa katika sura 1:2-4) katika ulimwengu huu. Hizi sifa nne ambazo zimo katika kundi la *sifaat tashbiihiyyah,* ni *Rabbil'aalamiin* (Mola wa walimwengu), *Ar-Rahmaan* (Mwingi wa rehema), *Ar-Rahiim* (Mwingi wa ukarimu) na *Maaliki yaumi-d-Diin* (Mmiliki wa siku ya Malipo).

Siku ya Kiyama sifa nne bora zinazolingana na hizo, yaani *sifaat tanziihiyyah,* zitafanya kazi. *Sifaat tashbiihiyyah* zinaweza kuitwa sifa za mshabaha, maana sifa hizo ni kama sifa zinazopatikana katika wanadamu. Mathalan, kama vile wafalme wanavyoonyesha ufalme wao kwa kukalia viti vyao vya enzi, kadhalika utukufu wa Allah uko katika kuwa kwake "Mola wa Arshi." Lakini siku ya Kiyama sifa hii itaonyesha sura yake iliyo bora, na hakuna kiumbe ye yote atakayeonyesha mfano wa sifa hiyo hata kidogo.

Baadhi ya wanazuoni wamefanya makosa kwa kuchukua ibara katika Aya nyingine za Qur'an ya kwamba Arshi ni kitu kilichoumbwa. Ibara hii inatolewa katika sura 69:18 miongoni mwa Aya nyinginezo, wakiwafanya Malaika "kubeba" kiti cha Enzi (Arshi) cha Allah. Kwa kukosa wanadhani ya kwamba maadamu Arshi inabebwa basi ni kitu chenye mwili.

Lakini hakika ni hii ya kuwa neno *haml* (kubeba) linatumiwa si kwa maana ya kubeba kitu chenye mwili tu, bali pia kwa mfano. Hivyo katika sura 33:73 mwanadamu anasemwa "anaibeba" Sheria aliyopewa na Mungu kama amana, hali sheria ya Mungu si kitu chenye mwili. Maneno hayo yana maana hii tu ya kwamba mwanadamu aliipokea sheria ya Mungu na akaifuata, na hivyo akasaidia kuibeba na kuiinua juu kwa kudhihirisha uzuri mwingi na ubora wa Sheria hiyo.

Hivyo, Malaika kubeba Arshi, mradi wake ni huu tu ya kwamba hakika yake inadhihirishwa na kubainishwa na Malaika. Ni wazi ya kwamba mtu hawezi kuelewa na kutambua sifa bora za Allah isipokuwa kwa njia ya sifa Zake za mshabaha, yaani, zile zinazodhihirika kwa kuhusiana na viumbe Vyake, ambazo viumbe nao wanazo. Hivyo, sifa za Allah zinazodhihirika kwa kuhusu viumbe Vyake ndizo, kama ilivyokuwa, zinazobeba sifa Zake zilizo bora, yaani, sifa za namna ya kwanza zinamsaidia mtu kufahamu na kutambua sifa za namna ya pili.

Aya nyingine inayowapa watu kufikiri ya kwamba Arshi imeumbwa, ni sura 23:87 inayom-

Ubishi unaletwa ya kwamba Allah ni *Rabb* (Mola) wa Arshi (kiti cha Enzi), hivyo lazima awe amekiumba. Lakini neno Rabb siyo lazima liwe na maana ya kuumba tu; pia maana yake ni mwenye kumiliki kitu au mwenye nacho. Hivyo, *Rabbul 'Arshi* litakuwa na maana ya "Mwenye kiti cha Enzi."

Katika sura 18:59 Allah amesemwa ni *Dhur-Rahma* (Mwenye rehema). Lakini rehema ni sifa ya Allah, si kiumbe. Hivyo, Mungu kusemwa ni Mwenye rehema, au Mwenye Arshi, haileti maana ya kwamba ni Mwumbaji wa hizo sifa Zake Mwenyewe.

Inaweza kuulizwa, ikiwa neno *Rabb* limetumiwa kwa maana ya *Dhuu* au *Saahib* (mwenye nacho au mwenyewe), kwa nini mojawapo katika hayo maneno mawili lisitumiwe badala ya neno *Rabb?* Jibu ni hili ya kwamba kutumia neno *Rabb* kumetimiza kusudi jingine moja. Baadhi ya Wanafalsfa wanamfanya Mungu kuwa ni chanzo cha kwanza tu.Kwao wao sifa za Allah zinaonekana zinajifanyia kazi zenyewe bila Yeye kuziongoza. Kwa hiyo, Qur'an imetumia neno *Rabb* (Mola) kwa kuhusiana na Arshi, ili kuonyesha ya kwamba sifa za Allah hazifanyi kazi zenyewe, bali zinafanya kazi kama atakavyo Allah, maana neno *Rabb* lina maana ya kuongoza pamoja na ile ya kuwa mwenye kitu.

Aya nyingine ambayo imekosewa kwa kuleta maoni ya kwamba Arshi ni kitu kilichoumbwa ni aya sura 11:8. Unaletwa ubishi ya kwamba kwa kuwa katika Aya hiyo Arshi inasemwa kuwa juu ya maji
ambayo ni kitu kilichoumbwa, hivyo Arshi nayo lazima iwe ni kitu kilichoumbwa.

Lakini ni lazima ikumbukwe ya kwamba neno "maji" katika sura 11:8 si maana yake maji haya ya kimwili. Arshi isingeweza kusemwa ilikuwa juu ya maji kabla ya kuumbwa mbingu na ardhi, maana maji ni sehemu ya ardhi na ni dhahiri yasingeweza kuwepo kabla ya kuumbwa ardhi. Tena, kiti cha kimwili kusemwa kilikuwa juu ya maji baada ya kuumbwa mbingu na ardhi hata haielekei.

Zaidi ya hayo, kwa kuwa maneno yote ya Mungu Mwenye hekima yamejaa busara sana, kuna kusudi gani kutueleza jambo lisilotuhusu? Kubainisha ya kwamba kiti cha Enzi cha Allah kilikaa juu ya maji hakudhihirishi utukufu wa Allah, maana hatuambiwi jinsi na namna kiti hiki kilivyokuwa kikikaa juu ya maji. Hivyo "maji" hapa si maana yake maji ya kimwili, wala "kiti cha Enzi" si mradi wake kiti cha kimwili. Kwa hakika katika usemi wa vitabu vilivyofunuliwa "maji" kila mara mradi wake ni wahyi, yaani neno la Mungu. Kwa maana hii Aya inafahamika hivi kuwa kiti cha Enzi cha Allah kinakaa juu ya neno la Allah, yaani mwanadamu hawezi kufahamu barabara ulivyo utukufu na Enzi ya Allah ila kwa kusaidiwa na wahyi ateremshao.

Kusema ya kwamba Arshi mradi wake ni sifa za Mungu zilizo bora pia ni jambo linalodhihirika katika sura 23:117 inayosema: *Hakuna aabudiwaye ila Yeye, Mola wa Kiti kitukufu cha Enzi.* Maneno haya yanaonyesha ya kwamba "umoja wa Allah" na "Kiti chake kitukufu cha Enzi" ni mambo mawili yanayoungana sana; maana ni sifa bora za Allah zinazotoa dalili hasa ya umoja wa Allah. Sifa nyingine watu wamezishiriki kwa kiasi mbalimbali, na inahitaji kuhoji kwa uhodari ili kumhakikishia mtu mwenye akili ya desturi umoja wa Allah kwa kutumia sifa hizi.

Hakuna mwombezi ila baada ya idhini Yake. Maneno haya yanafafanua habari ya uombezi ambayo imeelezwa katika sura 2:49 na 256. Itatosha hapa kueleza ya kwamba neno *Shafii'* limetoka katika neno *Shafa'* lenye maana ya kuunganisha pamoja vitu viwili vya namna moja. Kwa mujibu wa maana hii, itakuwa si sawa kusema ya kwamba kuamini uombezi kunaweza kumzidishia mtu mwovu katika madhambi kukimfikirisha kuwa haidhuru hata akifanya dhambi yuko wa kumwombea. Kufikiri hivi ni mbali kabisa na maana ya uombezi wa Kiislamu.

Kwa mafundisho ya Kiislamu, watakaoombewa ni wale tu walio wema ambao wamepungukiwa vitendo vyema vya kuwafikisha kwenye fadhili na rehema za Allah, na ambao kwa kiroho wameungana na Nabii Wake. Wala siyo hao waliozoea kufanya madhambi na kuvunja amri za Mungu makusudi, na hawana ufungamano wa kweli na Nabii Wake.

5. Kwake ndio marejeo yenu nyote. Ahadi ya Allah ni ya kweli. Hakika Yeye ndiye huanzisha kiumbe kisha Hukirudisha ili Awalipe walioamini na kufanya vitendo vizuri kwa adili. Lakini waliokufuru, wao watapata kinywaji cha maji yachemkayo na adhabu iumizayo kwa sababu walikuwa wakikataa.

6. Yeye Ndiye Aliyelifanya jua kuwa lenye kutoa mwanga na mwezi kuwa wenye nuru, na Akaukadiria vituo ili mjue idadi ya miaka na hesabu. Allah. Hakuviumba hivyo ila kwa haki. Huzieleza Ishara kwa watu wanaojua.

7. Hakika katika mfuatano wa usiku na mchana na Alivyoviumba Allah katika mbingu na ardhi ziko Ishara kwa watu waogopao.

اِلَيْهِ مَرْجِعُكُمْ جَمِيْعًا ؕ وَعْدَ اللّٰهِ حَقًّا ؕ
اِنَّهٗ يَبْدَؤُا الْخَلْقَ ثُمَّ يُعِيْدُهٗ لِيَجْزِيَ
الَّذِيْنَ اٰمَنُوْا وَعَمِلُوا الصّٰلِحٰتِ بِالْقِسْطِ ؕ
وَالَّذِيْنَ كَفَرُوْا لَهُمْ شَرَابٌ مِّنْ حَمِيْمٍ
وَّعَذَابٌ اَلِيْمٌۢ بِمَا كَانُوْا يَكْفُرُوْنَ ۝٤
هُوَ الَّذِيْ جَعَلَ الشَّمْسَ ضِيَآءً وَّالْقَمَرَ
نُوْرًا وَّقَدَّرَهٗ مَنَازِلَ لِتَعْلَمُوْا عَدَدَ السِّنِيْنَ
وَالْحِسَابَ ؕ مَا خَلَقَ اللّٰهُ ذٰلِكَ اِلَّا بِالْحَقِّ ۚ
يُفَصِّلُ الْاٰيٰتِ لِقَوْمٍ يَّعْلَمُوْنَ ۝٥
اِنَّ فِي اخْتِلَافِ الَّيْلِ وَالنَّهَارِ وَمَا خَلَقَ
اللّٰهُ فِي السَّمٰوٰتِ وَالْاَرْضِ لَاٰيٰتٍ لِّقَوْمٍ
يَّتَّقُوْنَ ۝٦

Aya 5. *Yeye Huanzisha kiumbe kisha Hukirudisha.* Kurudisha kiumbe kunakotajwa hapa kunahusu, kwanza, baada ya kufa mwanadamu atapewa uhai mpya, na katika uhai huo matendo yake aliyofanya hapa duniani yatalipwa; na pili, hata katika dunia hii vizazi vya wanadamu vinaandamana ili matendo mema ya kizazi kilichotakadamu (kilichotangulia) yasipotee bure na yawafae watu wa kizazi kinachowaandamia.

Neno *Saalihaat,* "Vitendo vizuri," baki ya kuwa na maana ya wema na utawa, pia maana yake ni vitendo vinavyofaa katika matukio vinamotendwa. Neno hili linaonyesha namna mtu au taifa linavyoweza kuendelea. Siyo kazi nzuri tu zinazopelekea mtu awe kwenye ustawi, bali matendo yanayofanywa katika wakati unaofaa sawa na mabadiliko ya hali na majira pia ni muhimu. Maangamio ya Waislamu wa leo yanatoa mfano unaofaa kuonyesha jinsi ilivyo hatari kudharau jambo hili la hakika. Katika wakati ilipohitajika juhudi ya kukuza vipawa vya akili, masheikh wa Kiislamu wasijali, wakashughulika na matendo ya nje ya ibada peke yake, wakapuuza shughuli nyingine zilizokuwa lazima kwa kuwapeleka mbele Waislamu.

Ilikuwa wajibu wao kuwatia Waislamu shauku kubwa ya kupenda kufanya kazi ili kuwafanya hodari na wenye nguvu, kuwafanya wenye mwenendo mzuri wa kuacha maovu yaliyokatazwa na dini, kuwahimiza kuwa stadi katika elimu na sanaa za kisasa, na kuwafunza namna ya kufanya kazi pamoja na watu wengine katika mambo yenye manufaa pande zote mbili. Lakini masheikh hawakufanya hivyo, na matokeo yake ni kwamba ibada zao peke yake hazikuweza kuwaponya. Vinavyoinua mataifa na kuyastawisha, zaidi huwa *Saalihaat,* yaani vitendo vizuri vinavyofanywa sawa na majira.

8. Hakika wale wasiotumaini kukutana nasi, na wamekuwa radhi na maisha ya dunia na kutulia kwayo, na wale pia wanaoghafilika na Aya Zetu;

اِنَّ الَّذِيْنَ لَا يَرْجُوْنَ لِقَآءَنَا وَرَضُوْا بِالْحَيٰوةِ الدُّنْيَا وَاطْمَاَنُّوْا بِهَا وَالَّذِيْنَ هُمْ عَنْ اٰيٰتِنَا غٰفِلُوْنَ ۙ﴿۷﴾

9. Hao ndio makazi yao ni Motoni kwa sababu ya yale waliyokuwa wakiyachuma.

اُولٰٓئِكَ مَاْوٰىهُمُ النَّارُ بِمَا كَانُوْا يَكْسِبُوْنَ ﴿۸﴾

10. Hakika wale walioamini na kufanya vitendo vizuri, Mola wao Atawaongoza kwa sababu ya imani yao. Itapita mito chini (ya miliki) yao katika Mabustani yenye neema.

اِنَّ الَّذِيْنَ اٰمَنُوْا وَعَمِلُوا الصّٰلِحٰتِ يَهْدِيْهِمْ رَبُّهُمْ بِاِيْمَانِهِمْ ۚ تَجْرِىْ مِنْ تَحْتِهِمُ الْاَنْهٰرُ فِىْ جَنّٰتِ النَّعِيْمِ ﴿۹﴾

Aya 8. Ni mtindo wa Qur'an kutumia maneno yanayoonekana mepesi lakini yenye namna nyingi za maana. Na kwa kuwa lugha ya Kiarabu ndio inayoweza zaidi kufanya kazi hii, Allah Ameipa heshima kuwa lugha ya Qur'an.

Neno *Rijaa* (kutumaini) ni mojawapo lenye maana zote mbili, kutumaini na kuogopa. Hivyo, kutumiwa neno hili katika Aya hii kumeipa ijae maana za undani sana.

Uchunguzi wa tabia za kibinadamu unadhihirisha jambo la maana sana ya kwamba maendeleo yote ya wanadamu yamefungamana na silika za tumaini na hofu. Baadhi ya watu wanafanya kazi na kutoka jasho wakishawishiwa na tumaini la kuchuma na kutukuka; wengine wanafanya kazi kwa hofu isije njaa ikawaletea mashaka. Aya hii inawapiga watu wa namna zote mbili. Wale ambao hutiwa ari ya kufanya kazi na tumaini, wanaambiwa, "Kwa nini hamtumaini kukutana na Allah, mkatengeneza mwenendo wenu kwa namna ya kuufaa mkutano huo, maana mafanikio yenu yote ya kidunia na ya kiakhera yanategemea mkutano huo." Na wale ambao hofu tu ndio inaweza kuwachochea kufanya kazi, Aya hii inawaambia, "Kwa nini hamuogopi na kujaribu kuepuka adhabu ya Allah, ambayo ikiwafikieni itawaangamizeni kabisa." Hivyo, kwa neno moja tu Qur'an imewahimiza watu wa namna zote mbili.

Wamekuwa radhi na maisha ya dunia na kutulia kwayo. Maneno haya yanaonyesha vizuri maoni ya Kiislamu juu ya maendeleo ya kidunia. Islam haikatazi kupata mafanikio ya kidunia. Isiyopendelea ni kwamba mtu afanye kuchuma vitu vya dunia hii ndio kazi hiyo tu aliyo nayo na asifikiri habari za Akhera.

Pili, Islam haipendelei ya kwamba mtu baada ya kupata mafanikio basi atulie kimya, na asijishughulishe kupata mafanikio zaidi. Kwa hakika kupata mema ya Akhera, pamoja na mafanikio ya kidunia, kunasemwa katika Qur'an kuwa moja katika fadhili za Allah, na kila Mwislamu anahimizwa kuomba kupata hayo (sura 2:202).

Wanaoghafilika na Aya Zetu. Maneno haya yanazidi kuhakikisha jambo hili, ya kwamba Allah Hapendezwi na hao tu wanaozama katika shughuli za kidunia na kutupilia mbali mambo ya kiroho.

Aya 10. *Mola wao Atawaongoza.* Maneno haya yanaonyesha ya kwamba mwongozo wa kweli unapatikana kwa kufuata imani ya kweli tu. Matendo matupu hayana thamani mpaka yamefuatana na utakaso wa moyo. Mtu anayetaka kuiba lakini hana nafasi ya kufanya hivyo, hawezi kuitwa mwaminifu. Kadhalika kama moyo wa mtu unaogopa vitu vingine visivyokuwa

دَعْوٰىهُمْ فِيْهَا سُبْحٰنَكَ اللّٰهُمَّ وَتَحِيَّتُهُمْ فِيْهَا سَلٰمٌ ۚ وَاٰخِرُ دَعْوٰىهُمْ اَنِ الْحَمْدُ لِلّٰهِ رَبِّ الْعٰلَمِيْنَ ۝١٠ ع ١

11. Wito wao humo utakuwa: Utakatifu ni Wako, Ee Allah, na maamkiano yao humo yatakuwa: Salaam. Na ilani yao ya mwisho itakuwa: Sifa zote njema zinamhusu Allah, Mola wa walimwengu.

FUNGU 2

وَلَوْ يُعَجِّلُ اللّٰهُ لِلنَّاسِ الشَّرَّ اسْتِعْجَالَهُمْ بِالْخَيْرِ لَقُضِيَ اِلَيْهِمْ اَجَلُهُمْ ؕ فَنَذَرُ الَّذِيْنَ لَا يَرْجُوْنَ لِقَآءَنَا فِيْ طُغْيَانِهِمْ يَعْمَهُوْنَ ۝١١

12. Na kama Allah Angaliwaharakishia watu shari kama wanavyojiharakishia kupata heri, bila shaka wangalitimiziwa muda wao. Lakini Tunawaacha wale wasiotumaini mkutano Wetu katika upotevu wao wakihangaika ovyo.

وَاِذَا مَسَّ الْاِنْسَانَ الضُّرُّ دَعَانَا لِجَنْۢبِهٖۤ اَوْ قَاعِدًا اَوْ قَآئِمًا ۚ فَلَمَّا كَشَفْنَا عَنْهُ ضُرَّهٗ مَرَّ كَاَنْ لَّمْ يَدْعُنَاۤ اِلٰى ضُرٍّ مَّسَّهٗ ؕ كَذٰلِكَ زُيِّنَ لِلْمُسْرِفِيْنَ مَا كَانُوْا يَعْمَلُوْنَ ۝١٢

13. Na dhara inapomgusa mtu, hutuita (anapolala) kibavu au katika hali ya kukaa au kusimama. Lakini Tunapomwondolea dhara yake hupita kana kwamba hakutuita juu ya dhara iliyomgusa. Hivyo ndivyo wamepambiwa warukao mipaka yale waliyokuwa wakiyatenda.

Lakini itakuwa si sawa kuchukua ibara katika Aya hii ya kwamba Islam haithaminishi vitendo vyema vya mtu na kufanya "imani" peke yake kuwa yatosha. Mkazo unaotiwa na Uislamu ni kwamba vitendo vyema lazima vifuatane na imani, yaani kutakasika moyo. Haiwezekani mtu mwenye moyo safi kukosa kutenda mema. Moyo wa mtu hautawaliwi na jambo lo lote la nje. Matendo yake yanaweza kutawaliwa lakini si moyo wake. Hivyo Allah ameufanya mwongozo utegemee juu ya kitu ambacho kiko kabisa katika uwezo wa mtu mwenyewe na ambacho hakitawaliwi kamwe na watu wengine. Hivyo kwa kuongeza maneno; *Kwa sababu ya imani yao,* Qur'an inagusia hakika ya kwamba vitendo vya mtu vitalipwa sawa na kiasi cha imani yake. Vitendo vya watu wawili vinaweza kuwa sawa na vyenye kupatana kwa mtazamo wa nje, lakini malipo yao yanaweza kuwa mbalimbali kabisa sawa na hitilafu ya vipimo vya imani yao, uaminifu wao na pendo lililowachochea kufanya vitendo hivyo. Kwa hakika jambo hili linafaa sana kukumbukwa.

Taht, "Chini." Neno hili limetumiwa kwa mfano kuonyesha kumiliki. Likichukuliwa kwa maana hii, maneno haya, chini yao, yataonyesha ya kwamba watu wa Peponi watamiliki mito hiyo na itakuwa mali zao wenyewe, na siyo kwamba wataitumia tu kwa kuruhusiwa hali si yao.

Aya 12. Aya hii inaonyesha ya kwamba wasioamini wameelekeza juhudi yao yote katika kuchuma mali na wamemwacha kabisa Allah. Hali hii inawaitia adhabu, lakini Allah hana haraka katika kutoa adhabu. Kama angekuwa anatoa adhabu mara

14. Na kwa yakini Tumekwisha viangamiza vizazi kabla yenu walipodhulumu; na waliwafikia Mitume wao kwa Ishara waziwazi; lakini hawakuwa wenye kuamini. Hivi ndivyo Tuwalipavyo watu wakosefu.

وَلَقَدْ اَهْلَكْنَا الْقُرُوْنَ مِنْ قَبْلِكُمْ لَمَّا ظَلَمُوْا ۙ وَجَآءَتْهُمْ رُسُلُهُمْ بِالْبَيِّنٰتِ وَمَا كَانُوْا لِيُؤْمِنُوْا ؕ كَذٰلِكَ نَجْزِى الْقَوْمَ الْمُجْرِمِيْنَ ﴿۱۳﴾

15. Kisha Tukawafanyeni mfuatao baada yao katika ardhi ili Tuone jinsi mtakavyotenda.

ثُمَّ جَعَلْنٰكُمْ خَلٰٓئِفَ فِى الْاَرْضِ مِنْۢ بَعْدِهِمْ لِنَنْظُرَ كَيْفَ تَعْمَلُوْنَ ﴿۱۴﴾

16. Na wanaposomewa Aya Zetu zilizo wazi, wale wasiotumai mkutano Wetu husema: Lete Qur'an isiyokuwa hii, au ibadilishe. Sema: Siwezi kuibadilisha kwa hiari ya nafsi yangu; sifuati ila yanayofunuliwa kwangu. Hakika mimi naogopa nikimwasi Mola wangu, adhabu ya siku iliyo kuu.

وَاِذَا تُتْلٰى عَلَيْهِمْ اٰيَاتُنَا بَيِّنٰتٍ ۙ قَالَ الَّذِيْنَ لَا يَرْجُوْنَ لِقَآءَنَا ائْتِ بِقُرْاٰنٍ غَيْرِ هٰذَآ اَوْ بَدِّلْهُ ؕ قُلْ مَا يَكُوْنُ لِىْٓ اَنْ اُبَدِّلَهٗ مِنْ تِلْقَآئِ نَفْسِىْ ۚ اِنْ اَتَّبِعُ اِلَّا مَا يُوْحٰٓى اِلَىَّ ۚ اِنِّىْٓ اَخَافُ اِنْ عَصَيْتُ رَبِّىْ عَذَابَ يَوْمٍ عَظِيْمٍ ﴿۱۵﴾

---

wanapostahili, wangekuwa wamekwisha angamizwa kabisa. Lakini Mungu huwapa watu muda wapate kutubu.

Kadhalika Aya hii iinaweza kutafsiriwa hivi, "Kama Allah Angaliwahimizia watu shari kama Anavyowahimizia heri, bila shaka wangalileteawa ajali yao;" lakini Allah ni Msamehevu, Mrehemevu, anawapa nafasi wapate kutubu.

Aya 14. *Al-Quruuna*, "Vizazi" Neno hili lina maana nyingi: (1) Sehemu ya wakati; (2) watu wa wakati mmojapo; (3) kizazi kinachokuja baada ya kingine; (4) watu wanaoangamizwa hata alama yao haibaki nyuma; (5) karne (Akrab na Lane).

Aya 15. Aya hii inaamsha swali moja lililo desturi, yaani watu hawaletwi mahali pa watu walioangamia ila baada ya kujulikana kuwa wale walioletwa nyuma watakuwa bora kuliko wao. Sasa kuna maana gani Allah kusena: *Ili Tuone jinsi mtakavyotenda?* Jibu la swali hili ni kwamba, matendo mema ni ya namna mbili: (1) Matendo yanayowapeleka watu kutukuka; (2) na matendo yanayotakiwa kuudumisha ule utukufu. Kuna watu wanaojiongoza vizuri hata kufikia ukubwa lakini baada ya kuupata hawawezi kudumisha mwenendo ulio bora katika watu wao, na wanakuwa wazembe na bila nidhamu. Zaidi ya hayo matendo ya watu yamegawanywa tena katika mafungu mawili zaidi. Baadhi ya vitendo ni vyema vyenyewe binafsi yao, ambapo vingine vinakuwa msingi wa kusimamishia vile vitendo vyema. Kwa kuongeza maneno haya, *Ili tuone jinsi mtakavyotenda,* Qur'an inataka kusema ya kuwa Mungu aliwafanyeni ninyi kuwa warithi wa fadhili Zake kwa sababu ya matendo yenu mema yaliyo ni chanzo kinachohitajiwa kwa kupata ukubwa; na sasa Mungu ataona jinsi mtakavyofanya matendo yale yanayouhifadhi ukubwa na kuudumisha.

Ukweli ni kwamba matendo mema ya namna ya pili ni magumu zaidi kutenda kuliko ya namna ya kwanza. Sababu mojawapo kubwa ya kuanguka mataifa ni kwamba ingawa wako tayari kupata kila namna ya taabu ili kupata heshima na ukubwa, hawafanyi juhudi kama hizo

17. Sema: Kama Allah Angalitaka nisingaliwasomeeni hiyo, wala Asingaliwajulisheni hiyo. Hakika nimekwisha kaa kati yenu umri mrefu kabla ya hayo, je, hamtumii akili.

قُلْ لَّوْ شَآءَ اللّٰهُ مَا تَلَوْتُهٗ عَلَيْكُمْ وَلَآ اَدْرٰىكُمْ بِهٖ ۖ فَقَدْ لَبِثْتُ فِيْكُمْ عُمُرًا مِّنْ قَبْلِهٖ ؕ اَفَلَا تَعْقِلُوْنَ ⑰

---

kudumisha tabia ya watu kuwa radhi kupata taabu na kuwa tayari kujinyima na kudumisha pendo la kutenda wema katika watoto wao. Hapo matokeo yanakuwa kwamba kizazi kimoja au zaidi waliostahili kinapofariki, basi uharibifu na ufisadi unawaingilia, hata mwishoni taifa zima linaangamia kabisa.

Kama Waislamu wangalitia kweli hii akilini, wasingetokomea katika shimo hili la dhila walimoangukia. Hata hivi sasa wakiitikia sauti ya Allah na kufuata fundisho la Aya hii, watapata tena utukufu wao uliokwisha potea.

Aya 17. *Hakika nimekwisha kaa kati yenu umri mwingi kabla ya hayo, je hamfahamu?* Maneno haya yana mizani mashuhuri ya kupimia madai ya mtu anayedai utume. Mtume *s.a.w* hapa anaambiwa awarejeshe makafiri kuangalia maisha yake aliyopitisha pamoja nao kuwa ndio dalili ya uaminifu wake na ukweli wake katika madai yake ya utume. Ikiwa maisha yake kabla ya kudai utume yalionyesha ni mtu mkweli kabisa na safi, na baina ya wakati ule na madai yake haukumpitia wakati wo wote unaoweza kusemwa kuwa alishuka toka hali ile ya juu ya tabia na mwenendo bora, basi madai yake ya kuwa Mtume lazima yakubaliwe kuwa yametoka kwa mtu mwenye tabia bora na mkweli.

Ilipokuwa hata maadui za Mtume walikiri kuwa maisha yake yote alikuwa peke yake mtu safi kabisa, hata wakampanga jina *al-Amin* (Mwaminifu), asingeweza kupinduka ghafla na kuwa mtu mbaya. Ingewezekanaje mtu aliyekuwa mnyofu kabisa na mwaminifu kati ya watu jana na leo awe mwongo mkubwa (kama asemavyo Mungu, Ni nani mdhalimu mkubwa kuliko yule amtungiaye Allah uwongo)? Kwa desturi mtu aliyezoea tabia namna fulani huchukua muda mrefu kujibadilisha kuwa mwema au mbaya. Inawezekanaje basi, Mtume Muhammad *s.a.w.* kupinduka ghafla na kuwa mwongo? Hapakuwa na wakati maisha yake yalipokuwa yamefichika mbele ya wenziwe. Alikuwa mwenyeji wa Makka, mtu wa kabila maarufu la Makka, akijulikana na wote kuwa ni *al-Amin* (Mwaminifu, mkweli). Hivyo juu ya tabia safi ya Mtume iliyojulikana sana, Qur'an inawaambia makafiri: "Mnamsingizia Mtume wetu uwongo mkubwa kupita kiasi ya kwamba anamtungia uwongo Allah, lakini hamwezi kutoa ushahidi wo wote kuonyesha mabadiliko hayo ya yeye kuwa mwovu yameanza lini kwake. Bali mnakiri wenyewe ya kwamba mpaka wakati alipodai utume aliendelea kuwa pamoja nanyi usiku na mchana, nanyi mlimwona ni mtu mkweli na mtawa wa namna ya pekee. Basi, mnawezaje sasa kusema ya kuwa ameanza ghafla kumtungia Mungu uwongo?"

Maneno haya, *Kabla ya hayo,* yanakusudiwa kuonyesha ya kwamba ubishi wa maadui za Mtume baada ya yeye kudai utume, watu wenye fikara nzuri wasiujali, maana imetokea kila siku mara mtu akidai kuwa yu Mtume wa Mungu, watu wanamgeuka na kumfanyia uadui, na wanaaza kumsingizia kila namna ya uovu. Mfalme Herakla (Emperor Heraclius) alifahamu sana nguvu ya hoja hii, na ndio maana Abu Sufyan alipopelekwa mbele yake huko Yerusalem, mfalme alimwuliza: Watu walimfikiriaje Mtume kabla hajadai utume? Abu Sufiyan alijibu ya kwamba watu walimfikiria kuwa mtu mkweli kabisa na mwema (Bukhari).

Maneno haya, *Je, hamfahamu?* yanatufahamisha ukweli wa mambo ya kimoyo unaojulikana sana ya kwamba mabadiliko ya ghafla hayamfikii mtu isipokuwa (1) kwa kujeruhiwa kiwiliwili n.k.w. (kama mtu amepigwa pigo la kichwa na limemtoa fahamu au kumbadilisha tabia n.k.w.),

فَمَنْ اَظْلَمُ مِمَّنِ افْتَرٰى عَلَى اللّٰهِ كَذِبًا اَوْ كَذَّبَ بِاٰيٰتِهٖ ؕ اِنَّهٗ لَا يُفْلِحُ الْمُجْرِمُوْنَ ﴿۱۷﴾

18. Basi ni nani mdhalimu mkubwa kuliko yule amtungiaye Allah uwongo, au akadhibishaye Aya Zake? Hakika wakosefu hawafaulu.

وَيَعْبُدُوْنَ مِنْ دُوْنِ اللّٰهِ مَا لَا يَضُرُّهُمْ وَلَا يَنْفَعُهُمْ وَيَقُوْلُوْنَ هٰٓؤُلَآءِ شُفَعَآؤُنَا عِنْدَ اللّٰهِ ؕ قُلْ اَتُنَبِّـُٔوْنَ اللّٰهَ بِمَا لَا يَعْلَمُ فِي السَّمٰوٰتِ وَلَا فِي الْاَرْضِ ؕ سُبْحٰنَهٗ وَتَعٰلٰى عَمَّا يُشْرِكُوْنَ ﴿۱۸﴾

19. Nao wanaabudu kinyume cha Allah yasiyoweza kuwadhuru wala kuwafaidisha; na wanasema: Hao ndio waombezi wetu mbele ya Allah. Sema: Je mtamwambia Allah Asiyoyajua katika mbingu wala katika ardhi? Ameepukana na upungufu, naye Yu juu sana kuliko wale wanaowashirikisha naye.

وَمَا كَانَ النَّاسُ اِلَّآ اُمَّةً وَّاحِدَةً فَاخْتَلَفُوْا ؕ وَلَوْلَا كَلِمَةٌ سَبَقَتْ مِنْ

20. Na watu hawakuwa ila kundi moja, lakini wakahitilafiana. Na kama si neno lililotangulia kutoka kwa Mola

---

msiba mzito ukamfanya mtu akate tamaa na kumfanya aelekee maovu; au kuvumbua ukweli mkubwa mtu akabadilika ghafla kuwa mwema. Tunapochungua habari za maisha ya Mtume *s.a.w* tunaona kwamba hakupatwa na mojapo katika mambo haya mawili. Kabla ya kupandishwa cheo cha utume alikaa maisha ya faragha, akimwomba Mungu na kufikiri. Papo kwa papo hakukata tamaa juu ya hali mbaya ya watu wa nchi yake na akiwatakia heri na kuwafanyia mema. Katika hali kama hizi ni kuitusi akili ya mtu na kuzitusi kanuni zote za elimu ya mambo ya moyo (psychology) kusema ya kwamba kabla hajadai utume Mtume Muhammad *s.a.w.* alikuwa mfano mwema wa utawa na mtu wa haki, lakini siku ile ile aliyodai utume akawa mwongo mkubwa kabisa! Kusema hivi ni jambo lisilokubalika hata kidogo.

Ushahidi uliotolewa na maadui za Mtume *s.a.w.*unahakikisha kabisa ya kuwa yeye alikuwa mtu mwema kabisa na mkweli kabisa hata kabla ya madai yake ya utume.

1. Abu Jahal, aliyekuwa adui mbaya kabisa wa Mtume *s.a.w.* siku moja alimwambia Mtume *s.a.w.,* "Hakika sisi hatusemi wewe u mwongo, bali tunasema uliyoyaleta ndio uwongo" (Tirmidhi, Kitabu *Tafsiir*).

2. Annadhar bin Haarith, aliyekuwa mmoja wa maadui tisa za Mtume *s.a.w.* waliopatana kumwua Mtume *s.a.w.*, safari moja makafiri walipokuwa wanashauriana wawaambie nini mahaji watakaofika Makka, juu ya Muhammad, mmoja wao akatoa shauri ya kwamba wawaambie ya kuwa Muhammad *s.a.w.* ni mwongo. Alisimama huyo Annadhar kwa hamaki na akasema, "Muhammad amekuwa kijana kati yenu, alikuwa mwenye tabia njema kuliko ninyi, alikuwa mkweli zaidi kuliko ninyi, na mwaminifu mkubwa, hata akaendelea katika hali hii mpaka mvi zimeanza kichwani mwake, na amewaleteeni ambayo amewaleteeni, na mmeanza kusema yeye ni mwongo? Wallahi huyu si mwongo" (Shifaa Kadhi Ayyadh).

3. Adui mwingine mkubwa wa Mtume *s.a.w.* aliyeitwa Umayya bin Khalf, kauli yake hii, "Wallahi Muhammad hasemi uwongo anaposema," inajulikana sana (Bukhari).

Aya 20. *Watu hawakuwa ila kundi moja, lakini wakahitilafiana.* Maneno haya yana maana tatu: (1) Ya kwamba Allah aliwafanya watu kufuata njia moja ya kweli mwanzo wa kuumbwa, lakini wakaiacha. Si kama Mungu alimpa mwanadamu uwezo wa kutambua njia iliyo

رَّبِّكَ لَقُضِيَ بَيْنَهُمْ فِيمَا فِيهِ يَخْتَلِفُونَ ﴿٢٠﴾

wako, bila shaka shauri lingekwisha katwa baina yao katika yale waliyohitilafiana.

وَيَقُولُونَ لَوْلَآ أُنزِلَ عَلَيْهِ ءَايَةٌ مِّن رَّبِّهِۦ ۚ فَقُلْ إِنَّمَا ٱلْغَيْبُ لِلَّهِ فَٱنتَظِرُوٓا ۚ إِنِّى مَعَكُم مِّنَ ٱلْمُنتَظِرِينَ ﴿٢١﴾ ع

21. Na wanasema: Kwa nini haikuteremshwa Ishara juu yake kutoka kwa Mola wake? Basi sema: Hakika yasiyoonekana ni ya Allah, kwa hiyo ngojeni; kwa yakini mimi ni pamoja nanyi katika wangojao.

FUNGU 3

وَإِذَآ أَذَقْنَا ٱلنَّاسَ رَحْمَةً مِّنۢ بَعْدِ ضَرَّآءَ مَسَّتْهُمْ إِذَا لَهُم مَّكْرٌ فِىٓ ءَايَاتِنَا ۚ قُلِ ٱللَّهُ أَسْرَعُ مَكْرًا ۚ إِنَّ رُسُلَنَا يَكْتُبُونَ مَا تَمْكُرُونَ ﴿٢٢﴾

22. Na Tunapowaonjesha watu rehema baada ya shida kuwagusa, lo! huanza kuzitungia hila Ishara Zetu. Sema: Allah ni mwepesi zaidi wa kujibu hila. Hakika Wajumbe Wetu wanaandika hila mnazozitunga.

هُوَ ٱلَّذِى يُسَيِّرُكُمْ فِى ٱلْبَرِّ وَٱلْبَحْرِ ۖ حَتَّىٰٓ إِذَا كُنتُمْ فِى ٱلْفُلْكِ ۖ وَجَرَيْنَ بِهِم بِرِيحٍ طَيِّبَةٍ وَفَرِحُوا۟ بِهَا جَآءَتْهَا رِيحٌ عَاصِفٌ وَجَآءَهُمُ ٱلْمَوْجُ مِن كُلِّ مَكَانٍ وَظَنُّوٓا۟ أَنَّهُمْ أُحِيطَ بِهِمْ ۙ دَعَوُا۟ ٱللَّهَ مُخْلِصِينَ لَهُ ٱلدِّينَ ۖ لَئِنْ أَنجَيْتَنَا مِنْ هَٰذِهِۦ لَنَكُونَنَّ مِنَ ٱلشَّٰكِرِينَ ﴿٢٣﴾

23. Yeye ndiye Anayewaendesheni katika bara na bahari, hata mnapokuwa katika merikebu na zinakwenda nao kwa upepo mzuri na wakajigamba nazo, upepo mkali unazifikia na mawimbi yanawajia toka kila upande, na wanaanza kufikiri ya kwamba wametingwa; (ndipo) wanamwomba Allah kwa kumhalisishia utii (wakisema): Ukituokoa katika haya, bila shaka tutakuwa miongoni mwa wanaoshukuru.

---

sawa tu, bali pia alimwelekeza kwenye njia hiyo kwa kumfunulia mwongozo; lakini mwanadamu akaiacha ile njia na kuangukia katika makosa. (2) Ya kwamba watu siku zote na kwa mfululizo wanaendelea kuonyeshwa njia iliyo sawa kwa kutumiwa Mitume, lakini tena wanaanza kuhitilafiana. Allah anamtuma mtu kuwa Mjumbe Wake miongoni mwao, na kwa kumfuata hivyo wanafikishwa kwenye njia ya haki, lakini tena wanaanza kuhitilafiana. (3) Ya kwamba makafiri kwa kumpinza Mtume wa Mungu siku zote wanashika hila za namna moja na hivyo wanakuwa kundi moja. Katika kila zama watu wamewapinza Mitume na wamehitilafiana nao.

Sehemu ya mwisho ya Aya inaonyesha ya kwamba kama Allah asingeweka kanuni ya kuwa siku zote hawaadhibu watu mpaka awapelekee Mtume, au isingekuwa ya kwamba amewaumba wanadamu ili wapate kuongoka na wapate maendeleo ya kiroho, angewaadhibu waovu upesi sana na kuwaangamiza.

فَلَمَّآ اَنْجٰىهُمْ اِذَا هُمْ يَبْغُوْنَ فِى الْاَرْضِ
بِغَيْرِ الْحَقِّ ؕ يٰٓاَيُّهَا النَّاسُ اِنَّمَا بَغْيُكُمْ
عَلٰٓى اَنْفُسِكُمْ ۙ مَّتَاعَ الْحَيٰوةِ الدُّنْيَا ۫ ثُمَّ
اِلَيْنَا مَرْجِعُكُمْ فَنُنَبِّئُكُمْ بِمَا كُنْتُمْ
تَعْمَلُوْنَ ﴿٢٤﴾

24. Lakini Anapowaokoa mara wanaanza kuasi katika ardhi bila haki. Enyi watu, uasi wenu utakuwa juu yenu tu, ni starehe ya maisha ya dunia, kisha marejeo yenu yatakuwa Kwetu, ndipo Tutawaambieni mliyokuwa mkiyafanya.

اِنَّمَا مَثَلُ الْحَيٰوةِ الدُّنْيَا كَمَآءٍ اَنْزَلْنٰهُ مِنَ
السَّمَآءِ فَاخْتَلَطَ بِهٖ نَبَاتُ الْاَرْضِ مِمَّا يَاْكُلُ
النَّاسُ وَالْاَنْعَامُ ؕ حَتّٰٓى اِذَآ اَخَذَتِ
الْاَرْضُ زُخْرُفَهَا وَازَّيَّنَتْ وَظَنَّ
اَهْلُهَآ اَنَّهُمْ قٰدِرُوْنَ عَلَيْهَآ ۙ اَتٰىهَآ
اَمْرُنَا لَيْلًا اَوْ نَهَارًا فَجَعَلْنٰهَا حَصِيْدًا
كَاَنْ لَّمْ تَغْنَ بِالْاَمْسِ ؕ كَذٰلِكَ نُفَصِّلُ
الْاٰيٰتِ لِقَوْمٍ يَّتَفَكَّرُوْنَ ﴿٢٥﴾

25. Hakika mfano wa maisha ya dunia ni kama maji Tuliyoyateremsha kutoka mawinguni, kisha mimea ya ardhi wanayokula watu na wanyama ikachanganyika nayo; hata ardhi ilipokamilisha uzuri wake na ikapambika, na wenyeji wake wakadhani kwamba wao wana nguvu juu yake, amri Yetu ikaifikia usiku au mchana na Tukaifanya imefyekwa, kana kwamba jana haikuwapo. Hivi ndivyo Tunavyoeleza Ishara kwa watu wanaofikiri.

وَاللّٰهُ يَدْعُوْٓا اِلٰى دَارِ السَّلٰمِ ؕ وَيَهْدِىْ مَنْ
يَّشَآءُ اِلٰى صِرَاطٍ مُّسْتَقِيْمٍ ﴿٢٦﴾

26. Na Allah Huita kwenye nyumba ya amani, na Humwongoza Amtakaye kwenye njia iliyonyooka.

لِلَّذِيْنَ اَحْسَنُوا الْحُسْنٰى وَزِيَادَةٌ ؕ وَلَا
يَرْهَقُ وُجُوْهَهُمْ قَتَرٌ وَّلَا ذِلَّةٌ ؕ اُولٰٓئِكَ
اَصْحٰبُ الْجَنَّةِ ۚ هُمْ فِيْهَا خٰلِدُوْنَ ﴿٢٧﴾

27. Wale waliofanya wema, watapata wema na zaidi; na vumbi halitawafunika nyuso zao wala fedheha. Hao ndio watu wa Peponi; humo watakaa.

Aya 25. Katika Aya hii maisha ya dunia hii yanafananishwa na mvua inayomwoteshea mtu mimea, kisha mtu anaanza kufikiri ameipata kwa ufundi wake. Basi balaa linapoifikia mimea yake, anashindwa kulizuia na kiburi chake hakifai kitu. Fumbo lililopo hapa ni kuwa mataifa yanapoanza kujivuna na kutakabari, basi kuanguka kwao kunawafikia na wanajuta.

Aya 26. *Salaam,* "Amani" ni ismu-feli ya neno *salama* lenye maana ya alisalimika; aliponyoka; amekuwa huru. Hivyo *Salaam* maana yake ni salama, hifadhi, kulindwa usipate kosa, upungufu, ila, waa au maovu; au maana yake ni salama tu au hifadhi; ulinzi; uhuru; amani; utii; Pepo. Pia ni moja katika majina ya Allah. (Akrab na Lane).

Hivyo maneno haya, *Allah Huita kwenye nyumba ya amani* pia yatakuwa na maana hizi: (1) Mungu ameweka utii kuwa sifa ya waaminio; na (2) Mungu amewafanya waaminio kuwa warithi wa baraka za Peponi; na (3) Mungu anawaweka waaminio wa kweli katika hali ya kumwona Mungu ana kwa ana.

Aya 27. *Al-Husnaa,* "Wema." Neno hili maana yake ni mwisho mwema, ushindi, uhodari na juhudi. Maneno ya Kiarabu yaliyofasiriwa, *Wale waliofanya wema watapata wema,* yatakuwa

وَالَّذِيْنَ كَسَبُوا السَّيِّاٰتِ جَزَآءُ سَيِّئَةٍ
بِمِثْلِهَا ۙ وَتَرْهَقُهُمْ ذِلَّةٌ ؕ مَا لَهُمْ مِّنَ
اللّٰهِ مِنْ عَاصِمٍ ۚ كَاَنَّمَاۤ اُغْشِيَتْ
وُجُوْهُهُمْ قِطَعًا مِّنَ الَّيْلِ مُظْلِمًا ؕ
اُولٰٓئِكَ اَصْحٰبُ النَّارِ ۚ هُمْ فِيْهَا خٰلِدُوْنَ ﴿٢٧﴾

28. Lakini wale waliochuma maovu, malipo ya uovu ni kama huo, na fedheha itawafunika. Hawatakuwa na awezaye kuwalinda na Allah; kana kwamba nyuso zao zimefunikizwa na kipande cha usiku wenye giza. Hao ndio watu wa Motoni, humo watakaa.

وَيَوْمَ نَحْشُرُهُمْ جَمِيْعًا ثُمَّ نَقُوْلُ لِلَّذِيْنَ
اَشْرَكُوْا مَكَانَكُمْ اَنْتُمْ وَشُرَكَآؤُكُمْ ۚ
فَزَيَّلْنَا بَيْنَهُمْ وَقَالَ شُرَكَآؤُهُمْ
مَّا كُنْتُمْ اِيَّانَا تَعْبُدُوْنَ ﴿٢٨﴾

29. Na siku Tutakayowakusanya wote, kisha Tutawaambia wale walioshirikisha: Simameni mahali penu ninyi na washirika wenu. Kisha Tutawatenga baina yao, na washirika wao watasema: Ninyi hamkuwa mkituabudu sisi.

فَكَفٰى بِاللّٰهِ شَهِيْدًا بَيْنَنَا وَبَيْنَكُمْ اِنْ
كُنَّا عَنْ عِبَادَتِكُمْ لَغٰفِلِيْنَ ﴿٢٩﴾

30. Basi Allah Atosha kuwa shahidi baina yetu na baina yenu. Hakika sisi tulikuwa hatuna habari ya ibada yenu.

هُنَالِكَ تَبْلُوْا كُلُّ نَفْسٍ مَّاۤ اَسْلَفَتْ
وَرُدُّوْۤا اِلَى اللّٰهِ مَوْلٰىهُمُ الْحَقِّ وَضَلَّ
عَنْهُمْ مَّا كَانُوْا يَفْتَرُوْنَ ﴿٣٠﴾ ع

31. Huko kila nafsi itayajua iliyoyatanguliza, na watarudishwa kwa Allah, Mola wao wa haki, na yatawapotea yale waliyokuwa wakiyatunga.

---

na maana ya kwamba waaminio watafikia mwisho wenye furaha; ya kwamba watafanikiwa, na ya kwamba Mungu atawafanya hodari na wenye juhudi.

Neno *Ziyaadah,* "Zaidi," linaonyesha ya kwamba waaminio watampata Mungu Mwenyewe kuwa malipo yao, neno *Al-Husnaa* (lenye pia maana ya kumwona Mungu) lakubaliana na ibara hii.

Aya 28. Aya hii imekusanya kweli nyingi zenye maana: (a) Ingawa ujira wa wema ni mwingi, ujira wa ubaya ni sawa na ubaya wenyewe; (b) wanaovunja Sheria ya Mungu wanakoma kupata mawazo bora na tamaa kubwa. Wanakuwa wenye kuigaiga wenzao, bila kuwa na uwezo wa kuanzisha mambo, na hawakusudii kuwa viongozi wa watu; (c) baada ya kuanguka hivi na kukosa radhi ya Mungu, wanakuwa hawaustahili msaada wa Allah ulio ni lazima kwa kuwanyanyua toka vilindi vya upotofu walimozama; (d) uovu na uasi wanaotenda waovu hauwezi kufichika kwa muda mrefu, bali sasa au baadaye lazima utaonekana bayana na kujulikana kwa watu.

FUNGU 4

قُلْ مَنْ يَّرْزُقُكُمْ مِّنَ السَّمَآءِ وَالْاَرْضِ اَمَّنْ يَّمْلِكُ السَّمْعَ وَالْاَبْصَارَ وَمَنْ يُّخْرِجُ الْحَيَّ مِنَ الْمَيِّتِ وَيُخْرِجُ الْمَيِّتَ مِنَ الْحَيِّ وَمَنْ يُّدَبِّرُ الْاَمْرَ ؕ فَسَيَقُوْلُوْنَ اللّٰهُ ۚ فَقُلْ اَفَلَا تَتَّقُوْنَ ﴿٣١﴾

32. Sema: Ni nani anayewaruzukuni kutoka mbinguni na ardhini? Au ni nani anayemiliki masikio na macho? Na ni nani amtoaye mzima katika mfu na kumtoa mfu katika mzima? Na ni nani atengenezaye mambo yote? Bila shaka watasema: Ni Allah. Basi sema: Je, hamumuogopi Allah?

فَذٰلِكُمُ اللّٰهُ رَبُّكُمُ الْحَقُّ ۚ فَمَاذَا بَعْدَ الْحَقِّ اِلَّا الضَّلٰلُ ۖۚ فَاَنّٰى تُصْرَفُوْنَ ﴿٣٢﴾

33. Basi Huyo Ndiye Allah, Mola wenu wa haki. Tena ni nini kinachobaki baada ya haki isipokuwa upotevu dhahiri? Basi mnageuzwa wapi?

كَذٰلِكَ حَقَّتْ كَلِمَتُ رَبِّكَ عَلَى الَّذِيْنَ فَسَقُوْٓا اَنَّهُمْ لَا يُؤْمِنُوْنَ ﴿٣٣﴾

34. Hivi ndivyo kauli ya Mola wako imehakiki juu ya wale walioasi, ya kwamba wao hawaamini.

قُلْ هَلْ مِنْ شُرَكَآئِكُمْ مَّنْ يَّبْدَؤُا الْخَلْقَ ثُمَّ يُعِيْدُهٗ ؕ قُلِ اللّٰهُ يَبْدَؤُا الْخَلْقَ ثُمَّ يُعِيْدُهٗ فَاَنّٰى تُؤْفَكُوْنَ ﴿٣٤﴾

35. Sema: Je, yuko katika washirikina wenu anayeanzisha kiumbe, kisha akakirejesha? Sema: Allah ndiye Aanzishaye kiumbe kisha Akakirejesha; basi mnageuzwa wapi?

قُلْ هَلْ مِنْ شُرَكَآئِكُمْ مَّنْ يَّهْدِيْٓ اِلَى الْحَقِّ ؕ قُلِ اللّٰهُ يَهْدِيْ لِلْحَقِّ ؕ اَفَمَنْ يَّهْدِيْٓ اِلَى الْحَقِّ اَحَقُّ اَنْ يُّتَّبَعَ اَمَّنْ لَّا يَهِدِّيْٓ اِلَّآ اَنْ يُّهْدٰى ۚ فَمَا لَكُمْ ۫ كَيْفَ تَحْكُمُوْنَ ﴿٣٥﴾

36. Sema: Je, yuko katika washirika wenu aongozaye kwenye haki? Sema: Allah ndiye Aongozaye kwenye haki. Basi Je, aongozaye kwenye haki anastahili zaidi kufuatwa au yule asiyeongoza isipokuwa aongozwe? Basi mmekuwaje? Mnahukumuje?

Aya 32. Aya hii inaeleza kwa namna nzuri jinsi ufunuo wa Allah unavyohusiana na akili: ni kama mvua na ardhi. Japo mvua ipige, kama ardhi haina hali njema, haiwezi kuotesha; na kadhalika ardhi yenye rutuba bila mvua ni kazi bure. Hivyo mtu hawezi kumfikia Mungu kwa akili zake tu bila kusaidiwa na wahyi wa Allah. Hapa mvua ni mfano wa wahyi au ufunuo na ardhi ni mfano wa akili ya mwanadamu.

37. Na wengi wao hawafuati ila dhana tu. Hakika dhana haifai mbele ya haki hata kidogo. Hakika Allah Anayajua wanayoyatenda.

وَمَا يَتَّبِعُ اَكْثَرُهُمْ اِلَّا ظَنًّا ؕ اِنَّ الظَّنَّ لَا يُغْنِىْ مِنَ الْحَقِّ شَيْـًٔا ؕ اِنَّ اللّٰهَ عَلِيْمٌۢ بِمَا يَفْعَلُوْنَ ﴿٣٧﴾

38. Na haiwezekani Qur'an hii kutungwa na ye yote isipokuwa Allah. Bali inayasadikisha yaliyo mbele yake, na ni maelezo ya Kitabu. Haina shaka ndani yake, imetoka kwa Mola wa walimwengu.

وَمَا كَانَ هٰذَا الْقُرْاٰنُ اَنْ يُّفْتَرٰى مِنْ دُوْنِ اللّٰهِ وَلٰكِنْ تَصْدِيْقَ الَّذِىْ بَيْنَ يَدَيْهِ وَتَفْصِيْلَ الْكِتٰبِ لَا رَيْبَ فِيْهِ مِنْ رَّبِّ الْعٰلَمِيْنَ ﴿٣٨﴾

Aya 37. *Dhanna,* "Dhana." Neno hili hutumika katika maana mbalimbali: (1) Shaka au kutokuwa na yakini; (2) wazo, fikira au kisio; (3) kuwa na sababu zenye nguvu pamoja na kukubali ya kwamba inawezekana jambo liwe kinyume na hivyo; (4) ujuzi au yakini (Lane).

Aya hii inataka kusema ya kwamba itikadi na maoni yanayoshikwa na washirikina yanatokana na dhana au shuku tu, kwa sababu miungu wao hawawafunulii mwongozo.

Kwa kutumia maneno, *wengi wao,* Qur'an haina maana ya kwamba baadhi ya washirikina wana sababu za kutosha kwa kushikilia miungu yao ya masanamu. Maneno hayo yametumiwa kuonyesha namna mbili za washirikina. Namna ya kwanza ni hao wanaoshikilia miungu yao ya masanamu kwa ajili ya choyo na ushupavu ingawa nyoyoni mwao wanajua vyema ya kuwa ibada ya masanamu haina msingi wa kweli au wenye akili. Namna ya pili, ambao ndio wengi, wanasadiki kwa roho safi kuwa miungu ni wengi, ingawa imani hiyo si kama wana sababu nayo au kukubaliwa na akili ama wameishika kwa kuichunguza,bali wanajifuatia tu kwa dhana na ushirikina.

Aya 38. Qur'an katika Aya hii inatoa sababu tano zenye nguvu sana kuonyesha ya kwamba bila shaka imetoka kwa Allah, na haikutungwa na mwanadamu.

1. Hoja ya kwanza inayodokezwa na maneno, *isipokuwa Allah,* ni ya kwamba Qur'an ina habari za namna ambayo zimekiuka akili ya mwanadamu kuzijua, na haziwezi kubainishwa ila na Allah peke yake. Sasa katika mambo yanayojulikana na Allah peke yake, ni habari za mambo ya ghaibu, kama bishara zinazotaja matukio makubwa ya baadaye; na hapawezi kuwa shaka juu ya Kitabu kutoka kwa Mungu chenye habari anazozijua Mungu peke yake.

2. Hoja ya pili inayotolewa hapa kuonyesha kuwa Qur'an imetoka kwa Allah ni kwamba mbali na bishara zake yenyewe, kubatilisha wazo la kusema imetungwa na mtu, bishara za Manabii waliotangulia pia zinahakikisha kuwa Qur'an imetoka kwa Mungu. Jambo hili linagusiwa katika maneno haya, *inayasadikisha yaliyo mbele yake,* na ni wazi ya kwamba hakuna kitabu kinachotungwa na mwanadamu kinachoweza kujitimizia bishara zilizotabiriwa katika Vitabu vya Manabii waliopita zamani.

3. Hoja ya tatu iliyomo katika Aya hii inagusiwa na maneno haya *Maelezo ya Kitabu,* yaani Qur'an inaeleza na kutoa tafsiri ya mafundisho ya Vitabu vya zamani. Hii pia ni dalili yenye nguvu sana ya ukweli wa Qur'an. Vitabu vilivyotangulia vinahitaji msaada wa Qur'an kwa kufafanua mafundisho yao. Taurati, Injili, Vedas, Zend-Avesta - vyote hivi ni vitabu vya zamani vinavyoshughulika kueleza mafumbo makubwa makubwa ya mambo ya dini kama vile umoja wa Allah, wahyi na ufunuo, sifa za Allah, utume, maisha ya Akhera, hali za tabia na za roho n.k.w. Lakini hakuna kimoja katika vitabu hivyo kinachoeleza mambo haya kwa namna ya kuyafanya yawe wazi kabisa na kufahamika, na mitatanisho yao ni lazima ielezwe kwa msaada wa mafundisho ya Qur'an.

39. Je, wanasema ameitunga? Sema: Basi leteni sura moja mfano wake na waiteni mwezao badala ya Allah, kama ninyi mnasema kweli.

اَمْ يَقُوْلُوْنَ افْتَرٰىهُ ؕ قُلْ فَاْتُوْا بِسُوْرَةٍ مِّثْلِهٖ وَادْعُوْا مَنِ اسْتَطَعْتُمْ مِّنْ دُوْنِ اللّٰهِ اِنْ كُنْتُمْ صٰدِقِيْنَ ﴿۳۹﴾

40. Bali wameyakadhibisha wasiyoyazunguka elimu yake wala hakika yake haijawafikia. Hivi ndivyo walikadhibisha waliokuwa kabla yao. Basi angalia jinsi ulivyokuwa mwisho wa wadhalimu.

بَلْ كَذَّبُوْا بِمَا لَمْ يُحِيْطُوْا بِعِلْمِهٖ وَلَمَّا يَاْتِهِمْ تَاْوِيْلُهٗ ؕ كَذٰلِكَ كَذَّبَ الَّذِيْنَ مِنْ قَبْلِهِمْ فَانْظُرْ كَيْفَ كَانَ عَاقِبَةُ الظّٰلِمِيْنَ ﴿۴۰﴾

Hivyo Aya hii inaleta madai ya kwamba Qur'an inaeleza na kufafanua sehemu za vitabu vya zamani zisizofahamika vyema na zenye kutatiza; na makafiri wanaambiwa ya kwamba kama watakataa Qur'an kutoka kwa Mungu, watalazimika kukubali ya kwamba Mungu mwenyewe hakuweza kutia elimu nyingi ya mambo ya kiroho katika Vitabu vya zamani kama alivyoweza mwanadamu (Mtume Muhammad) kufanikiwa kutia katika hiki Kitabu kidogo tu cha Qur'an. Hivyo wafuasi wa dini nyingine watalazimika ama kukubali Qur'an imetoka kwa Mungu au kukataa Vitabu vya zamani pia.

4. Hoja ya nne katika Aya hii imo katika maneno, *Haina shaka,* yaani Qur'an ina hoja zote na dalili zote zinazotakikana kuthibitisha kuwa imetoka kwa Mungu, na haina haja ya kusaidiwa na mtu nje au kitabu kingine kwa jambo hilo. Qur'an inaeleza migogoro ya maisha ya watu kukaa pamoja, ya mwenendo na tabia na ya mambo ya kiroho, kwa ukamilifu na utoshelezo wa namna ambayo mtu ye yote atakayeifikiria bila upendeleo ataona mara moja ya kuwa Qur'an haitoi madai yo yote ila inayafuatisha na hoja madhubuti, na dalili imara. Jambo hili ni ushahidi usiokanushika ya kwamba Kitabu hiki bila shaka kimetoka kwa Mungu; maana Qur'an inataka tuamini mambo mengi yasiyoonekana, na haiko katika uwezo wa mwanadamu kuhakikisha mambo yasiyoonekana kwa hoja za akili tu bila kusaidiwa na uwezo wa kutazama na mazoea. Lakini ni wazi mtu hawezi kuviangalia vitu visivyoonekana na kuvizoea. Mungu tu ndiye awezaye kufanya hivyo.

5. Hoja ya tano ya kuhakikisha kuwa Qur'an imetoka kwa Mungu inayoelezwa na Aya hii imo katika maneno haya, *Imetoka kwa Mola wa walimwengu.* Maneno haya yanadokeza ya kwamba kwa Qur'an hii sifa ya Allah ya *Rabbul 'Aalamiin* (Mola wa walimwengu) imedhihirishwa kwa wanadamu wote. Qur'an haikusudiwi kutosheleza mahitaji ya taifa mojawapo au majira fulani tu, kama ilivyokuwa hali ya Vitabu vilivyotangulia; bali inakusudiwa kutosheleza haja za mataifa yote na za nyakati zote. Kwa hakika haiwezekani kwa mwanadamu kutoa Kitabu kinachoweza kutosheleza haja za wanadamu wote kwa nyakati zote. Kwa desturi mtu huvutwa na mastakimu yake naye huangalia na kutaka kutosheleza haja zake zilizo karibu naye. Ni Mungu peke yake anayeweza kutoa mafundisho ya namna ambayo yawe yanafaa sawasawa kila wakati na kwa watu wote, ambayo hayawezi kuhafifishwa na mabadiliko ya nyakati na hali. Basi Qur'an ndio ina mafundisho ya namna hiyo.

Aya 39. Licha ya uzuri wa Qur'an uliotajwa katika Aya iliyotangulia, makafiri walikuwa bado na ujasiri wa kusema ya kwamba Qur'an imetungwa na Mtume *s.a.w.* Aya hii inawauliza, kama Kitabu bora namna hiki kinaweza kutungwa na mwanadamu, basi kwa nini makafiri nao hawajitungii chao kimoja cha namna hii? Wito wa mashindano kama haya umetangazwa katika Qur'an mahali mbalimbali. Mahali pamoja makafiri wameambiwa walete Kitabu kinachofanana na Qur'an nzima; mahali pengine wameambiwa walete sura kumi zinazoweza kulinganishwa na sura za Qur'an; na bado mahali pengine Qur'an imewataka walete hata sura moja inayofanana na sura za Qur'an. Jambo hili linaonyesha ya kwamba kila fungu lenye wito huo wa mashindano hayo, linatoa wito wa namna ya peke yake na kila wito ni mbali na mwingine.

41. Na miongoni mwao yuko anayeiamini, na miongoni mwao yuko asiyeiamini. Na Mola wako Awajua sana waharibifu.

وَمِنْهُمْ مَّنْ يُّؤْمِنُ بِهٖ وَمِنْهُمْ مَّنْ لَّا يُؤْمِنُ بِهٖ ؕ وَرَبُّكَ اَعْلَمُ بِالْمُفْسِدِيْنَ ﴿٤١﴾ ع ۹

FUNGU 5

42. Na kama wakikukadhibisha, basi sema: Mimi nina amali yangu na ninyi mna amali yenu; nanyi hamhusiki na niyatendayo, wala mimi sihusiki na yale mnayoyatenda.

وَاِنْ كَذَّبُوْكَ فَقُلْ لِّيْ عَمَلِيْ وَلَكُمْ عَمَلُكُمْ ۚ اَنْتُمْ بَرِيْٓـُٔوْنَ مِمَّآ اَعْمَلُ وَاَنَا بَرِيْٓءٌ مِّمَّا تَعْمَلُوْنَ ﴿٤٢﴾

Mathalan neno "wake" katika tamko *mithlihii* (mfano wake) haliihusu Qur'an yote, bali linahusu tu Aya iliyoitangulia hii. Kama ambavyo tumeona Aya hiyo imeleta hoja tano kuhakikisha ya kwamba Qur'an ni neno la Mungu lililofunuliwa, na katika Aya hii makafiri wanaambiwa kama bado wanashikilia kuidhani Qur'an ni neno la mwanadamu, basi nao walete Kitabu ambacho, wacha mbali shauri ya kuwa na dalili zote tano zilizomo katika Aya iliyotangulia, chao kiwe haidhuru na dalili moja tu. Ni jambo la hakika kabisa ya kwamba hakuna hata dalili moja katika hizi tano, zithubutishazo Qur'an kutoka kwa Mungu, inayoweza kupatikana katika kitabu cho chote kilichotungwa na mwanadamu. Haya ndio madai ambayo hakuna ye yote aliyethubutu kuyapinza, wala haiwezekani kuwa hata baadaye atatokea awezaye kuyapinza. Wito huu wa mashindano unasimama kwa nyakati zote. Mbingu na ardhi vinaweza kuondoka, lakini hakuna mtu atakayeweza kuleta kitabu mfano wa Qur'an.

Kama neno *Suura* katika Aya hii lichukuliwe kwa maana ya sura, hapo Aya hii itakuwa na maana ya kwamba makafiri wanatakiwa walete hata sura moja inayofanana na Qur'an. Lakini hapo mashindano hayataonyeshwa hivyo. Maana katika sura hiyo makafiri wataitwa kuleta sura nzima yenye dalili zote tano zilizotajwa katika Aya iliyotangulia, ambapo katika hali ya kwanza wanatakiwa walete utungo wo wote wenye sifa tu ya hizo tano. Pia tazama sura 2:24.

Aya 41. Aya hii inaonyesha ya kwamba, maadui, juu ya uadui wao, si kama wote hawataongoka. Baadhi yao watarudi nafsi zao na kukubali Uislamu. Wale tu wanaoshikilia mwendo mbaya na wanaoendelea kutenda maovu mpaka mwisho ndio watajinyima kabisa imani na mwongozo. Aya inaeleza sababu kwa nini adhabu ya Mungu iliakhirishwa, ya kwamba si kama ilielekea tu kuwa baadhi yao wataingia Uislamu, bali Allah alijua barabara kuwa wengine wao watakuwa Waislamu waaminifu kabisa. Hivyo akaacha kuwapelekea adhabu Yake mapema.

Aya hii ina bishara kubwa iliyotimizwa baadaye. Kama watu wa Makka wangehilikishwa mara moja walipomkataa Mtume, watu kama Khalid bin Waliid na 'Amir bin al-A'as, 'Ikrima bin Abu Jahal na watetezi wengine wengi hodari wa Uislamu wangekubalije dini ya haki?

Aya 42. Aya hii inabainisha vizuri jinsi Islamu ilivyo kwa ajili ya watu wote na ilivyo na mawazo mapana. Makafiri wanaambiwa hapa ya kwamba kama wanapendelea kumkataa Mtume, wako huru kabisa kufanya hivyo. Kwa kweli kila inapotokea hitilafu baina ya maoni ya makundi mawili, kila kundi lina haki ya kuonyesha kuwa jingine ndilo lenye makosa. Lakini hitilafu hii isiruhusiwe kuruka mipaka, na kundi mojapo lisishurutishe wenzao kukubali tu vile watakavyo wao.

43. Na wako miongoni mwao wanaokusikia sana. Je, unaweza kuwasikilizisha viziwi ingawa hawana akili?

وَمِنْهُمْ مَّنْ يَّسْتَمِعُوْنَ اِلَيْكَ ؕ اَفَاَنْتَ تُسْمِعُ الصُّمَّ وَلَوْ كَانُوْا لَا يَعْقِلُوْنَ ﴿٤٢﴾

44. Na wako miongoni mwao wanaokutazama. Je, unaweza kuwaongoza vipofu ingawa hawaoni?

وَمِنْهُمْ مَّنْ يَّنْظُرُ اِلَيْكَ ؕ اَفَاَنْتَ تَهْدِى الْعُمْىَ وَلَوْ كَانُوْا لَا يُبْصِرُوْنَ ﴿٤٣﴾

45. Hakika Allah Hawadhulumu watu cho chote, lakini watu wanajidhulumu wenyewe.

اِنَّ اللّٰهَ لَا يَظْلِمُ النَّاسَ شَيْـًٔا وَّلٰكِنَّ النَّاسَ اَنْفُسَهُمْ يَظْلِمُوْنَ ﴿٤٤﴾

46. Na siku Atakayowakusanya (wataona) kana kwamba hawakukaa (duniani) ila saa moja tu ya mchana; watajuana wao kwa wao. Hakika wamekwisha pata hasara wale waliokadhibisha kukutana na Allah, wala hawakuwa wenye kuongoka.

وَيَوْمَ يَحْشُرُهُمْ كَاَنْ لَّمْ يَلْبَثُوْٓا اِلَّا سَاعَةً مِّنَ النَّهَارِ يَتَعَارَفُوْنَ بَيْنَهُمْ ؕ قَدْ خَسِرَ الَّذِيْنَ كَذَّبُوْا بِلِقَآءِ اللّٰهِ وَمَا كَانُوْا مُهْتَدِيْنَ ﴿٤٥﴾

47. Na kama Tukikuonyesha baadhi ya yale Tunayoyaonya au Tukufishe kabla, marejeo yao ni Kwetu, kisha Allah Atakuwa Shahidi juu ya yale wanayoyatenda.

وَاِمَّا نُرِيَنَّكَ بَعْضَ الَّذِىْ نَعِدُهُمْ اَوْ نَتَوَفَّيَنَّكَ فَاِلَيْنَا مَرْجِعُهُمْ ثُمَّ اللّٰهُ شَهِيْدٌ عَلٰى مَا يَفْعَلُوْنَ ﴿٤٦﴾

Aya hii inasema ya kwamba inapojulikana vyema ya kuwa waaminio na makafiri ni makundi mawili mbalimbali na hakuna maelekeo ya kukosa kuwapambanua, na inapokuwa namna zao za kufanya kazi pia ni tofauti, basi hakuna sababu ya kutumia nguvu. Nguvu inaweza kutumiwa inapokuwa mwendo wa kundi moja unaelekea kulitia aibu kundi jingine. Lakini wanapokuwa kama walivyo, matendo ya Mtume na wafuasi wake hayatii aibu upande wa makafiri, wala matendo ya makafiri hayatii aibu upande wa waaminio, basi kundi mojapo halina haki ya kuwaletea karaha wengine.

Aya hii pia inaweza kufasiriwa namna nyingine. Inaweza kuwa na maana ya kwamba matendo ya Mtume *s.a.w.* yanapambanuka kabisa mbali na yale ya makafiri, na hayashabihiani. Basi, mambo yawapo kama hivyo, matokeo yataonyesha ni kazi ya nani iliyo sawa na ya nani yenye makosa. Kunapokuwa mfanano baina ya matendo ya pande mbili, ni vigumu kupambanua sababu ya maendeleo au maanguko ya kundi mojapo lo lote. Lakini kunapokuwa hakuna mshabaha japo katiti baina ya matendo ya pande mbili, basi kila mtu anapata usemeo yanapoonekana matokeo.

Aya 47. Aya hii imeweka kanuni ya jambo la maana ya kwamba bishara zenye maonyo na matisho ya kufika adhabu zinaweza kuachwa zisitimizwe. Aya hii inaonyesha ya kwamba bishara huwa za namna mbili: (1) Zenye masharti, kama inavyobainika katika neno *immaa* (kama) na *aw* (au) yaliyotumiwa katika Aya hii; (2) zinazoweza kuvunjwa au kuzuiwa zisitimizwe, kama linavyoonyesha neno *ba'adh* (baadhi) na *nuriyannaka* (Tukikuonyesha). Neno *ba'adh* linaonyesha wazi kabisa ya kwamba Aya hii inasema juu ya bishara zile tu zilizokusudiwa

وَلِكُلِّ اُمَّةٍ رَّسُوْلٌ ۚ فَاِذَا جَآءَ رَسُوْلُهُمْ قُضِيَ بَيْنَهُمْ بِالْقِسْطِ وَهُمْ لَا يُظْلَمُوْنَ ﴿٤٧﴾

48. Na kila umati una Mtume. Basi anapofika Mtume wao inahukumiwa baina yao kwa uadilifu nao hawadhulumiwi.

وَيَقُوْلُوْنَ مَتٰى هٰذَا الْوَعْدُ اِنْ كُنْتُمْ صٰدِقِيْنَ ﴿٤٨﴾

49. Na husema: Lini ahadi hii (itatimia) kama mnasema kweli?

قُلْ لَّآ اَمْلِكُ لِنَفْسِيْ ضَرًّا وَّلَا نَفْعًا اِلَّا مَا شَآءَ اللّٰهُ ؕ لِكُلِّ اُمَّةٍ اَجَلٌ ؕ اِذَا جَآءَ اَجَلُهُمْ فَلَا يَسْتَاْخِرُوْنَ سَاعَةً وَّلَا يَسْتَقْدِمُوْنَ ﴿٤٩﴾

50. Sema: Similiki kwa ajili ya nafsi yangu hasara wala faida, isipokuwa Apendayo Allah. Kila umati una muda. Unapofika muda wao, basi hawataikawia saa wala hawataitangulia.

قُلْ اَرَءَيْتُمْ اِنْ اَتٰىكُمْ عَذَابُهٗ بَيَاتًا اَوْ نَهَارًا مَّاذَا يَسْتَعْجِلُ مِنْهُ الْمُجْرِمُوْنَ ﴿٥٠﴾

51. Sema: Mwaonaje kama iwafikieni adhabu Yake usiku au mchana, wataikimbiaje wenye makosa?

اَثُمَّ اِذَا مَا وَقَعَ اٰمَنْتُمْ بِهٖ ؕ آٰلْـٰٔنَ وَقَدْ كُنْتُمْ بِهٖ تَسْتَعْجِلُوْنَ ﴿٥١﴾

52. Je, ikisha tokea mtaiamini? Je, sasa! na hali mlikuwa mkiiharakishia.

ثُمَّ قِيْلَ لِلَّذِيْنَ ظَلَمُوْا ذُوْقُوْا عَذَابَ الْخُلْدِ ۚ هَلْ تُجْزَوْنَ اِلَّا بِمَا كُنْتُمْ تَكْسِبُوْنَ ﴿٥٢﴾

53. Kisha waliodhulumu wataambiwa, Ionjeni adhabu idumuyo. Hamtalipwa ila kwa yale mliyokuwa mkiyachuma.

---

dhahiri hazikukusudiwa kutimizwa bado angali hai, na hivyo hazikuhitaji zitajwe katika maneno haya tuliyo nayo. Kwa bahati Aya hii pia inaonyesha ya kuwa inayumkinika bishara yo yote ya adhabu isitimizwe Mtume bado angali hai, maana iliwezekana ya kwamba wote wale aliokuwa anawahubiria Uislamu, wamwamini, na hivyo kusingekuwa sababu ya kufika adhabu. Maneno ya Aya hii pia yamepangwa kwa namna ya kuonyesha uwezo kamili wa Allah; waila, kwa desturi sio watu wote huamini.

Aya hii pia inaonyesha ya kwamba si lazima bishara ziwekewe muda wa kuzitimiza, kwani muda uliowekwa kwa kutimizwa bishara zilizosemwa hapa haukuwekewa kipimo, ukivuka hata kuingia katika nyakati za baada ya kufariki Mtume *s.a.w.* Naam, hata kama muda uonekane kama umewekwa, ambao hapa utakuwa maadamu Mtume yu hai. Muda wenye kikomo silo jambo kubwa kwani Aya yenyewe inakubali ya kwamba sehemu ya bishara hizi haitatimia katika wakati wa uhai wa Mtume *s.a.w.*

Zaidi ya hayo inajitokeza katika Aya hii ya kwamba bishara zinazoweza kutanguliwa na kuvunjwa ni zile tu zinazohusu mambo yasiyo muhimu, maana bishara zinazohusu kanuni zilizo kubwa za daima, hizo hazivunjwi. Mfano wa bishara za aina isiyotanguka ni huu: *Allah Ameandika: Bila shaka Nitashinda Mimi na Mitume Wangu*. (sura 58:22); ilhali bishara zinazotanguliwa ni kama zinazobainishwa na Aya hii tunayoieleza isemayo, *yale Tunayowaonya.* Hii inaonyesha ya kwamba bishara zenye matisho na maonyo juu ya adhabu inayokaribia huenda zikavunjwa, ambapo zile zenye ahadi ya mambo ya desturi, yanayohusu Mitume wote wa Mungu, haziwezi kattu kuvunjwa, na ni lazima zitimie.

54. Na wanakuuliza: Je, ni kweli hiyo? Sema: Ehe! naapa kwa Mola wangu, hiyo ni kweli, nanyi hamwezi kumuajizisha Allah.

وَيَسْتَنْۢبِـُٔوْنَكَ اَحَقٌّ هُوَ ؕ قُلْ اِىْ وَرَبِّىْٓ ۙ اِنَّهٗ لَحَقٌّ ۚ وَمَآ اَنْتُمْ بِمُعْجِزِيْنَ ﴿٥٤﴾ ع ١٣ ١٠

FUNGU 6

55. Na kama kila mtu aliyedhulumu angalikuwa na (yote) yaliyomo ardhini, bila shaka angeyatoa kujikomboa. Na watakapoiona adhabu wataficha majuto; na itahukumiwa baina yao kwa uadilifu, nao hawatadhulumiwa.

وَلَوْ اَنَّ لِكُلِّ نَفْسٍ ظَلَمَتْ مَا فِى الْاَرْضِ لَافْتَدَتْ بِهٖ ؕ وَاَسَرُّوا النَّدَامَةَ لَمَّا رَاَوُا الْعَذَابَ ۚ وَقُضِىَ بَيْنَهُمْ بِالْقِسْطِ وَهُمْ لَا يُظْلَمُوْنَ ﴿٥٥﴾

56. Sikilizeni! bila shaka vilivyomo katika mbingu na ardhi ni vya Allah. Sikilizeni! hakika ahadi ya Allah ni haki, lakini wengi wao hawajui.

اَلَآ اِنَّ لِلّٰهِ مَا فِى السَّمٰوٰتِ وَالْاَرْضِ ؕ اَلَآ اِنَّ وَعْدَ اللّٰهِ حَقٌّ وَّلٰكِنَّ اَكْثَرَهُمْ لَا يَعْلَمُوْنَ ﴿٥٦﴾

57. Yeye ndiye Huhuisha na Hufisha, na Kwake mtarejeshwa.

هُوَ يُحْىٖ وَيُمِيْتُ وَاِلَيْهِ تُرْجَعُوْنَ ﴿٥٧﴾

58. Enyi watu! hakika yamewafikieni mawaidha kutoka kwa Mola wenu na tiba ya yale yaliyomo vifuani, na mwongozo na rehema kwa waaminio.

يٰٓاَيُّهَا النَّاسُ قَدْ جَآءَتْكُمْ مَّوْعِظَةٌ مِّنْ رَّبِّكُمْ وَشِفَآءٌ لِّمَا فِى الصُّدُوْرِ ۙ وَهُدًى وَّرَحْمَةٌ لِّلْمُؤْمِنِيْنَ ﴿٥٨﴾

Aya 53. *'Adhaabal-khuldi,* "Adhabu ikaayo." Mradi wake ni adhabu itakayokuja kaa na kuwapasukia wasioamini; si mradi wake adhabu isiyo na mwisho. Neno hili linaonyesha namna

Aya 55. *Asarrunnadaamat,* "Wataficha majuto." Maneno haya pia yanaweza kutafsiriwa, "Watadhihirisha majuto."

Aya 56. Aya hii inaonyesha ukweli ulio mkuu. Kwa kuwa vyote vilivyomo mbinguni na duniani ni vya Allah, ni kazi bure kujaribu kumpendeza Mungu au Mtume Wake kwa kuwapa rushwa (tazama Aya iliyotangulia). Mitume wa Mungu hawawezi kuzuiwa kuendesha ujumbe waliotumwa kwa ajili ya rushwa. Watu wa Makka wakijaribu kumzuia Mtume s.a.w. asihubiri kulaumu ibada ya masanamu, walitaka kumpa kila namna ya rushwa; lakini juu ya rushwa zao zote aliwajibu ya kwamba hata kama wakiweka jua juu ya mkono wake wa kulia, na mwezi mkono wake wa kushoto, hataacha ujumbe wake (Hisham na Zurkani).

Hakika ni kwamba kwa kuwa masultani na wafalme wanahitaji vitu vya dunia hii, basi rushwa na vitu vya kujikombolea vinawapendeza. Lakini kwa kuwa Mungu mwenyewe ndiye Mwumba wa vitu vyote, vitu vya kujikombolea havina thamani Kwake isipokuwa mtu ajitoe sadaka yeye mwenyewe, hapo Mungu kwa haraka anapokea, kwani sadaka ya namna hiyo ni njia ya kujitakasa.

Aya 58. Aya hii inaonyesha ni kwa sababu gani Mtume *s.a.w.* alishinda upesi. Inaeleza ya kwamba si majeshi ya vita wala makasiki ya mali au makundi ya wafuasi bali ni Qur'an iliyo

59. Sema: Kwa fadhili za Allah na rehema Zake, basi wafurahie hayo. Hiyo ni bora kuliko wanavyovikusanya.

قُلْ بِفَضْلِ اللّٰهِ وَ بِرَحْمَتِهٖ فَبِذٰلِكَ فَلْيَفْرَحُوْا ؕ هُوَ خَيْرٌ مِّمَّا يَجْمَعُوْنَ ﴿۵۹﴾

60. Sema: Je mmeona Aliyowateremshieni Allah katika riziki kisha mkafanya katika hiyo haramu na halali. Sema: Je, Allah Amewaruhusuni, au mnamtungia Allah uwongo?

قُلْ اَرَءَيْتُمْ مَّاۤ اَنْزَلَ اللّٰهُ لَكُمْ مِّنْ رِّزْقٍ فَجَعَلْتُمْ مِّنْهُ حَرَامًا وَّ حَلٰلًا ؕ قُلْ آٰللّٰهُ اَذِنَ لَكُمْ اَمْ عَلَى اللّٰهِ تَفْتَرُوْنَ ﴿۶۰﴾

61. Na ni nini dhana ya wale wanaomtungia Allah uwongo juu ya siku ya Kiyama? Hakika Allah ndiye Mwenye kuwafadhili watu, lakini wengi wao hawashukuru.

وَمَا ظَنُّ الَّذِيْنَ يَفْتَرُوْنَ عَلَى اللّٰهِ الْكَذِبَ يَوْمَ الْقِيٰمَةِ ؕ اِنَّ اللّٰهَ لَذُوْ فَضْلٍ عَلَى النَّاسِ وَلٰكِنَّ اَكْثَرَهُمْ لَا يَشْكُرُوْنَ ﴿۶۱﴾ ع ۱۲

FUNGU 7

62. Na hushughuliki katika kazi yo yote, wala husomi humo katika Qur'an, wala hamfanyi kitendo cho chote,

وَمَا تَكُوْنُ فِيْ شَاْنٍ وَّمَا تَتْلُوْا مِنْهُ مِنْ قُرْاٰنٍ وَّلَا تَعْمَلُوْنَ مِنْ عَمَلٍ اِلَّا كُنَّا

---

bora, na mafundisho yake yenye nguvu, ambayo mtu hawezi kushindana nayo kwa muda mrefu ila yatamwathiri, na atakuwa radhi kuyageukia yamwongoze.

Qur'an ni mauidha kwa sababu ina mafundisho ambayo yamekuja kwa nia safi ya kuwapa watu shauri jema. Hivyo, watu wanapoona ya kwamba Mtume hatafuti kujitukuza kwa kutangaza mafundisho haya, bali anachotaka ni kwamba wapone, hawatakosa kuvutwa na mafundisho yake; (b) mafundisho ya Qur'an yamefanywa kwa namna ambayo yanazama mpaka kuuathiri moyo wa mtu. Yanatia mkazo sana juu ya kumpenda na kumwogopa Mungu hata mtu mwenye moyo mgumu sana hawezi kubakia yasimwathiri; (c) yameweka kwa namna nzuri kila kanuni na sheria ya tabia njema zinazomsahihisha mtu na kumfanikisha.

Kama Aya hii inavyotuambia, Qur'an ni *Shifaa* (uponyi) pia. Qur'an inaponya magonjwa yote ya kiroho. Mtu na awe ameanguka namna gani, akili yake huendelea kuwa na kiu ya ukweli, na kutaka kujua hakika ya mambo. Na ni pale akili yake inapokuwa inavurugwa na shaka, naye anataka kupata utulivu juu ya mambo ya kiroho, ndipo Qur'an inajitokeza kumponya na kuondoa shaka zake zote; na matokeo yanakuwa ya kwamba inamvuta sana aipende.

Qur'an ni "ponyo" la yale yaliyomo moyoni kwa maana ya kwamba inatosheleza matamanio ya moyo. Ni tabia ya mwanadamu anaposoma habari za watu wakubwa katika dini, na kujua jinsi vina virefu vya mambo ya kiroho vilivyofunguliwa kwao, roho yake inatamani ya kwamba mambo hayo anayoyasadiki yawe pia kwa ajili yake aone kama vile watu watakatifu wa zamani walivyoona. Hii ndio tamaa inayosumbua mioyo ya watu wengi, na watu ambao nyoyo zao zimeshikwa na tamaa hii watapata maburudiko katika Kitabu hiki, na ndani yake wataona mwongozo utakaowafikisha kwa Allah.

Aya 62. Aya hii ni mojawapo katika Aya mashuhuri za Qur'an. Inaonekana kana kwamba

عَلَيْكُمْ شُهُوْدًا اِذْ تُفِيْضُوْنَ فِيْهِ ؕ وَمَا يَعْزُبُ عَنْ رَّبِّكَ مِنْ مِّثْقَالِ ذَرَّةٍ فِي الْاَرْضِ وَلَا فِي السَّمَآءِ وَلَاۤ اَصْغَرَ مِنْ ذٰلِكَ وَلَاۤ اَكْبَرَ اِلَّا فِيْ كِتٰبٍ مُّبِيْنٍ ﴿٦١﴾

اَلَاۤ اِنَّ اَوْلِيَآءَ اللّٰهِ لَا خَوْفٌ عَلَيْهِمْ وَلَا هُمْ يَحْزَنُوْنَ ﴿٦٢﴾

isipokuwa Sisi Tunakuwa mashahidi juu yenu mnaposhughulika nayo. Wala hakifichikani kwa Mola wako kitu cho chote kilicho sawa na uzito wa chembe katika ardhi wala katika mbingu, wala kidogo kuliko hicho wala kikubwa, isipokuwa kimo katika Kitabu kielezacho.

63. Sikilizeni! hakika marafiki wa Allah hawana hofu wala hawahuzuniki.

Allah Anatoa hotuba Yake penye Kiti Chake cha Enzi na Utukufu. Na upande Wake mmoja yuko Mtume Muhammad *s.a.w*. pamoja na wafuasi wake, na upande mwingine kuna makafiri. Maneno haya *na hushughuliki katika kazi yo yote, wala husomi humo katika Qur'an,* yanaambiwa Mtume Muhammad na Waislamu, na maneno haya, *Wala hamfanyi kitendo cho chote, isipokuwa Sisi Tunakuwa mashahidi juu yenu mnaposhughulika nayo,* yanaambiwa makafiri. Aya hii inawakumbusha waaminio ya kwamba kukubali haki peke yake au kubashiri dini peke yake, si mambo yenye kutosha. Kinachotakikana ni namna mtu anavyoiingiza imani yake katika matendo yake, na nia inayompeleka kufanya matendo hayo. Kwa hiyo mumini wa kweli anatakiwa kila mara kuchungua barabara nia yake na matendo yake. Hivyo, walioamini wasijidanganye bure kuwa kujisema kwao wameamini na kuitangaza imani hiyo kutawapatia radhi ya Allah na kuwavutia msaada Wake. Wanalazimika kuonyesha kwa usafi wa nia zao na wema wa matendo yao ya kwamba kweli wanastahili kibali cha Allah. Aya hii inatoa somo kubwa la kwamba isipokuwa matendo mema yatendwe kwa nia njema na kwa namna nzuri, hayawezi kuleta matokeo mema au kumpatia mtu radhi ya Allah.

Upande mwingine makafiri wanapewa onyo kali ya kwamba kukataa kwao haki na kuicheka na kuidhihaki, na pia matendo yao ya kuipinza dini ya Mungu, hayapiti bila kuonekana, nao watakutana na ajali inayowastahili.

Maneno haya *asghar* na *akbar* (kidogo na kikubwa), yametumiwa kuonyesha ya kwamba, kuna baadhi ya vitu vinafichikana kwa sababu ya udogo wao, na kuna vingine vinakuwa vikubwa sana hata kwa kiasi cha kufanya sehemu zao nyingine zisionekane. Kwa mfano, mtu anaweza kuona sehemu tu ya mlima mkubwa wala si wote. Kwa hiyo Qur'an inasema sawa ya kwamba nguvu ya kuona ya Allah ni kali kabisa hata hakuna kitu kiwe kidogo namna gani kinaweza kufichama asikione. Na pia nguvu Yake ya kuona imeenea kabisa hata kitu kiwe kikubwa chapataje hakuna sehemu yake yo yote itakayokaa asiione.

Kadhalika elimu ya *sayansi* imehakikisha ya kwamba kuona na kusikia kunategemea mitingisho *(vibrations)* yenye kikomo. Kuna kikomo cha jicho kuona na sikio kusikia. Nguvu ile inapopungua au kuzidi kiasi kinachotakiwa, jicho halitaona wala sikio halitasikia. Kwa mfano, sikio haliwezi kusikia sauti iliyo si chapu chapu kuliko mitingisho *(vibrations)* thelathini kwa nukta moja; wala haliwezi kusikia sauti iliyo kasi zaidi ya mitingisho *(vibrations)* arobaini kwa nukta moja. Hivyo, hata elimu ya *sayansi* imehakikisha ya kwamba baadhi ya vitu vinaliponyoka jicho au sikio kwa sababu ya ima udogo wao au ukubwa wao. Lakini Qur'an inasema, hivyo sivyo mambo yalivyo kwa Allah ambaye anaviona vitu vyote kwa ukamilifu, vidogo au vikubwa.

Aya 63. *Laa khaufun 'alaihim,* "Hawana hofu" Maana ya maneno haya ni kwamba

اَلَّذِيْنَ اٰمَنُوْا وَكَانُوْا يَتَّقُوْنَ ﴿٦٣﴾

64. Ambao waliamini na wakawa wamchao.

لَهُمُ الْبُشْرٰى فِي الْحَيٰوةِ الدُّنْيَا وَفِي الْاٰخِرَةِ ؕ لَا تَبْدِيْلَ لِكَلِمٰتِ اللّٰهِ ؕ ذٰلِكَ هُوَ الْفَوْزُ الْعَظِيْمُ ﴿٦٤﴾

65. Wao wanazo habari njema katika maisha ya dunia na katika Akhera. Hakuna mabadiliko katika maneno ya Allah; huo ndio ufaulu mkubwa.

وَلَا يَحْزُنْكَ قَوْلُهُمْ ۘ اِنَّ الْعِزَّةَ لِلّٰهِ جَمِيْعًا ؕ هُوَ السَّمِيْعُ الْعَلِيْمُ ﴿٦٥﴾

66. Wala isikuhuzunishe kauli yao. Hakika utukufu wote ni wa Allah. Yeye Ndiye Asikiaye, Ajuaye.

اَلَاۤ اِنَّ لِلّٰهِ مَنْ فِي السَّمٰوٰتِ وَمَنْ فِي الْاَرْضِ ؕ وَمَا يَتَّبِعُ الَّذِيْنَ يَدْعُوْنَ مِنْ دُوْنِ اللّٰهِ شُرَكَآءَ ؕ اِنْ يَّتَّبِعُوْنَ اِلَّا الظَّنَّ وَاِنْ هُمْ اِلَّا يَخْرُصُوْنَ ﴿٦٦﴾

67. Sikilizeni! bila shaka vilivyomo mbinguni na ardhini ni vya Allah. Na wale wanaowaomba washirika badala ya Allah kwa hakika hawawafuati hao washirika. Bali wanafuata dhana tu na hawasemi ila uwongo tu.

---

waaminio hawahofu kuwa kuna dhara yo yote ya hakika itakayowafika. Maneno haya siyo maana yake kuwa hakuna hatari itakayowafikia. Kadhalika maneno, *Walaa hum yahzanuun,* "Wala hawatahuzunika," maana yake ni kuwa waaminio hawatapata huzuni juu ya yale waliyoyatenda zamani. Hivyo, yajayo na yaliyopita yamewekwa salama kwa ajili ya waaminio. Hali hii ya ajabu, maana hakuna ufalme wo wote duniani unaoweza kuahidi kwa yakini kulinda salama ya mtu ya mambo yake yaliyopita na ya baadaye. Ni Allah tu anayeweza kufanya hilo. Kwa hakika inasikitisha ya kwamba badala ya watu kumgeukia Allah ili wawe salama wanageukia ambako hawawezi kuipata salama.

Maneno *khauf* (hofu) na *Huzn* (huzuni) kwa yakini yametumiwa katika Qur'an katika matukio fulani juu ya Manabii. Lakini hofu au huzuni ya Manabii huwa si juu yao wao wenyewe, bali huwa kwa kuwaonea wengine, na kuwahofia watu wengine au kuwahuzunikia ni jambo la kusifiwa, si adhabu. Ni kwa maana hii neno *huzn* (huzuni) limetumiwa kwa ajili ya Nabii Yakubu katika sura 12:85, na neno *khauf* (hofu) likatumiwa kwa ajili ya Nabii Zakaria katika sura 19:6.

Aya 65. *Wanazo habari njema.* Mtume s.a.w. alisema ya kuwa hizi habari njema ni "Ndoto za kweli zinazomhusu mumini anazoziona, au ambazo watu wengine wanaziona zinazomhusu yeye" (Bukhari). Neno *Bushraa* (habari njema) lina matumizi mapana na linaweza kutumiwa kwa kuhusu wahyi na njozi za Manabii, pia za mawalii na waaminio; na Aya hii inahusu namna zote hizi mbili za njozi na wahyi (Jarir na Kathir).

Hakuna mabadiliko katika maneno ya Allah. Maneno haya yanaweza kuwa na maana mbili: (a) Kuleta *bushraa* (habari njema) ni sheria ya Allah na ya tangu azali, na kwa kuwa ni ya azali basi itawatimilia Waislamu pia; na (b) hii ni ahadi maalumu wanayopewa Waislamu, na Allah amekata shauri ya kwamba ahadi hii haitabadilika. Jambo hili linaonyesha ya kwamba kuna baadhi ya bishara zisizoingia katika kundi la "maneno ya Mungu" yaliyotajwa katika Aya hii, na ambazo zinaweza kubadilishwa, na ziko nyingine zinazoingia katika kundi hilo na ambazo

هُوَ الَّذِیْ جَعَلَ لَكُمُ الَّیْلَ لِتَسْكُنُوْا فِیْهِ وَالنَّهَارَ مُبْصِرًا ؕ اِنَّ فِیْ ذٰلِكَ لَاٰیٰتٍ لِّقَوْمٍ یَّسْمَعُوْنَ ﴿۶۸﴾

68. Yeye ndiye Aliyewafanyieni usiku ili humo mtulie, na mchana ung'aao. Hakika katika hayo zimo Ishara kwa watu wasikiao.

قَالُوا اتَّخَذَ اللّٰهُ وَلَدًا سُبْحٰنَهٗ ؕ هُوَ الْغَنِیُّ ؕ لَهٗ مَا فِی السَّمٰوٰتِ وَمَا فِی الْاَرْضِ ؕ اِنْ عِنْدَكُمْ مِّنْ سُلْطٰنٍ بِهٰذَا ؕ اَتَقُوْلُوْنَ عَلَی اللّٰهِ مَا لَا تَعْلَمُوْنَ ﴿۶۹﴾

69. Wanasema: Allah Amepanga mwana! Ameepukana na hayo, Yeye Anajitosheleza. Ni vyake vilivyomo mbinguni na vilivyomo ardhini. Ninyi hamna dalili kwa hayo. Je, mnasema juu ya Allah msiyoyajua?

قُلْ اِنَّ الَّذِیْنَ یَفْتَرُوْنَ عَلَی اللّٰهِ الْكَذِبَ لَا یُفْلِحُوْنَ ﴿۷۰﴾

70. Sema: hakika wale wanaomsingizia Allah uwongo hawafaulu.

مَتَاعٌ فِی الدُّنْیَا ثُمَّ اِلَیْنَا مَرْجِعُهُمْ ثُمَّ نُذِیْقُهُمُ الْعَذَابَ الشَّدِیْدَ بِمَا كَانُوْا یَكْفُرُوْنَ ﴿۷۰﴾ ع ۱۲

71. Watapata manufaa katika dunia. Kisha marejeo yao ni Kwetu. Ndipo Tutawaonjesha adhabu kali, kwa sababu walikuwa wakikufuru.

FUNGU 8

وَاتْلُ عَلَیْهِمْ نَبَاَ نُوْحٍ ۘ اِذْ قَالَ لِقَوْمِهٖ یٰقَوْمِ اِنْ كَانَ كَبُرَ عَلَیْكُمْ مَّقَامِیْ وَتَذْكِیْرِیْ بِاٰیٰتِ اللّٰهِ فَعَلَی اللّٰهِ تَوَكَّلْتُ فَاَجْمِعُوْۤا اَمْرَكُمْ وَشُرَكَآءَكُمْ ثُمَّ لَا یَكُنْ اَمْرُكُمْ عَلَیْكُمْ غُمَّةً ثُمَّ اقْضُوْۤا اِلَیَّ وَلَا تُنْظِرُوْنِ ﴿۷۱﴾

72. Na uwasomee habari za Nuhu alipowaambia watu wake: Enyi watu wangu! ikiwa cheo changu na kukumbusha kwangu Aya za Allah yanawachukizeni, basi mimi namtegemea Allah. Basi kusanyeni nguvu zenu zote na washirika wenu, kisha msiwe na shaka yoyote juu ya nguvu zenu, kisha nifanyieni chochote mwezacho.

فَاِنْ تَوَلَّیْتُمْ فَمَا سَاَلْتُكُمْ مِّنْ اَجْرٍ ؕ اِنْ اَجْرِیَ اِلَّا عَلَی اللّٰهِ ۙ وَاُمِرْتُ اَنْ اَكُوْنَ مِنَ الْمُسْلِمِیْنَ ﴿۷۲﴾

73. Lakini mkigeuka, basi siwaombeni ujira. Ujira wangu hauko ila kwa Allah; na nimeamrishwa niwe miongoni mwa wajisalimishao.

فَكَذَّبُوْهُ فَنَجَّیْنٰهُ وَمَنْ مَّعَهٗ فِی الْفُلْكِ وَجَعَلْنٰهُمْ خَلٰٓئِفَ وَاَغْرَقْنَا الَّذِیْنَ كَذَّبُوْا

74. Lakini wakamkadhibisha, na Tukamuokoa yeye na waliokuwa naye katika merikebu, na Tukawafanya wairithi nchi na Tukawaza-

بِاٰيٰتِنَا ۚ فَانْظُرْ كَيْفَ كَانَ عَاقِبَةُ
الْمُنْذَرِيْنَ ﴿٧٤﴾

misha wale waliozikadhibisha Ishara Zetu. Basi angalia jinsi ulivyokuwa mwisho wa wale walioonywa!

ثُمَّ بَعَثْنَا مِنْۢ بَعْدِهٖ رُسُلًا اِلٰى قَوْمِهِمْ
فَجَآءُوْهُمْ بِالْبَيِّنٰتِ فَمَا كَانُوْا لِيُؤْمِنُوْا
بِمَا كَذَّبُوْا بِهٖ مِنْ قَبْلُ ؕ كَذٰلِكَ نَطْبَعُ عَلٰى
قُلُوْبِ الْمُعْتَدِيْنَ ﴿٧٥﴾

75. Kisha Tukawatuma Mitume baada yake kwa watu wao, nao wakawafikia kwa Ishara waziwazi, lakini hawakuwa wenye kuyaamini waliyoyakadhibisha zamani. Hivi ndivyo Tunavyopiga muhuri juu ya mioyo ya watu warukao mipaka.

ثُمَّ بَعَثْنَا مِنْۢ بَعْدِهِمْ مُّوْسٰى وَهٰرُوْنَ
اِلٰى فِرْعَوْنَ وَمَلَا۟ئِهٖ بِاٰيٰتِنَا فَاسْتَكْبَرُوْا
وَكَانُوْا قَوْمًا مُّجْرِمِيْنَ ﴿٧٦﴾

76. Kisha baada ya hao Tukawatuma Musa na Harun kwa Firauni na wakuu wake na Ishara Zetu, lakini wakajivuna, nao walikuwa watu wakosefu.

فَلَمَّا جَآءَهُمُ الْحَقُّ مِنْ عِنْدِنَا قَالُوْٓا اِنَّ
هٰذَا لَسِحْرٌ مُّبِيْنٌ ﴿٧٧﴾

77. Basi ilipowafikia haki kutoka Kwetu wakasema: Bila shaka huu ndio uchawi dhahiri.

Aya 75. Aya hii inaonyesha bayana kabisa ya kwamba si Allah anayeifunga mioyo ya makafiri, bali ni makafiri wenyewe ambao kwa ushupavu wao wa kukataa bila haki kusikiliza maneno ya Allah, wanauharibu uwezo wao wa kuiona haki na kuikubali. Wao wenyewe ndio wamejitengenezea mwisho wao mbaya, na Allah amepiga muhuri kuhakikisha kuwa kweli wana hali hiyo waliyojitengenezea wenyewe. Jambo la kupiga muhuri mioyo ya makafiri linasemwa ni la Allah kwa sababu Yeye ndiye Hakimu wa Mwisho anayekata hukumu.

Aya 76. Nabii wa Allah hukataliwa na watu kwa sababu mbili. Ama kwa kuwa watu anaowabashiria ujumbe wake wanaona madai yake ni makubwa mno, wakifikiri kwamba Mungu hawezi kusema na mtu; au kwa sababu ya kiburi wanaona watavunja heshima zao wakimfuata. Jambo hili lilitokea kwa Nabii Musa. Baadhi ya watu aliowabashiria walikataa madai yake kwa sababu walifikiri kuwa haikuwezekana Allah ajishushe kwa kusemezana na mwanadamu; wengine waliona ni kinyume na heshima zao kumtii mtu mdogo kama Musa.

Aya 77. *Sihr,* "Uchawi." Neno hili maana yake ni kutoa kilicho uwongo kwa sura ya ukweli, kupamba kitu kwa uwongo na udanganyifu; ulozi au uchawi (Lane). Pia tazama sura 7:110.

Mubiin, "Dhairi." lina maana tatu: (1) dhahiri bayana au wazi; (2) kitu kinachofanya kitu kiwe bayana au dhahiri; (3) kitu kinachotenganisha, kufarikisha, na kukosanisha (Lane).

Maneno haya mawili *sihr* na *mubiin* yanaonyesha kila namna ya hila wanayotumia maadui wa Nabii wa Mungu ili kuharibu kazi yake. Watu wenye akili inayoelekea kwenye dini wanaambiwa na maadui hao ya kwamba haya mafundisho mapya si cho chote ila ni *sihr* tu. yaani udanganyifu ambao utaharibu dini inayofuatwa na watu tangu zamani katika nchi; na watu wenye kutakia heri nchi yao wanaogopeshwa nao kwa kuambiwa kuwa haya mafundisho mapya ni *mubiin*, yaani kuyakubali kutaleta mfaraka katika nchi na kuleta ugomvi baina ya jamii mbalimbali za watu na

78. Akasema Musa: Je, mnasema (hivi) juu ya haki ilipowafikieni? Je, huu ni uchawi? Na wachawi hawastawi.

قَالَ مُوْسٰٓى اَتَقُوْلُوْنَ لِلْحَقِّ لَمَّا جَآءَكُمْ ؕ اَسِحْرٌ هٰذَا ؕ وَلَا يُفْلِحُ السّٰحِرُوْنَ ﴿۷۸﴾

79. Wakasema: Je, umetujia ili utuondoe katika yale tuliyowakuta nayo baba zetu, na ili ukubwa uwe wenu wawili katika nchi? Na sisi hatuwezi kuwaamini.

قَالُوْٓا اَجِئْتَنَا لِتَلْفِتَنَا عَمَّا وَجَدْنَا عَلَيْهِ اٰبَآءَنَا وَتَكُوْنَ لَكُمَا الْكِبْرِيَآءُ فِى الْاَرْضِ ؕ وَمَا نَحْنُ لَكُمَا بِمُؤْمِنِيْنَ ﴿۷۹﴾

80. Na Firauni akasema: Nileteeni kila mchawi hodari.

وَقَالَ فِرْعَوْنُ ائْتُوْنِىْ بِكُلِّ سٰحِرٍ عَلِيْمٍ ﴿۸۰﴾

81. Basi walipofika wachawi, Musa akawaambia: Tupeni mnavyotaka kuvitupa.

فَلَمَّا جَآءَ السَّحَرَةُ قَالَ لَهُمْ مُّوْسٰٓى اَلْقُوْا مَآ اَنْتُمْ مُّلْقُوْنَ ﴿۸۱﴾

82. Na walipotupa, Musa akasema: Mliyoleta ni udanganyifu tu wa macho; hakika Allah hivi karibuni Ataubatilisha. Hakika Allah Hastawishi vitendo vya waharibifu.

فَلَمَّآ اَلْقَوْا قَالَ مُوْسٰى مَا جِئْتُمْ بِهِ ۙ السِّحْرُ ؕ اِنَّ اللّٰهَ سَيُبْطِلُهٗ ؕ اِنَّ اللّٰهَ لَا يُصْلِحُ عَمَلَ الْمُفْسِدِيْنَ ﴿۸۲﴾

83. Na Allah Ataimarisha haki kwa maneno Yake, ingawa wakosefu wachukie.

وَيُحِقُّ اللّٰهُ الْحَقَّ بِكَلِمٰتِهٖ وَلَوْ كَرِهَ الْمُجْرِمُوْنَ ﴿۸۳﴾ ع ۱۳

---

na hivyo kazi ya taifa kwenda mbele itaharibika.Upanga huu wenye makali kuwiali ndio uliotumiwa kila mara kwa kuwapinza Mitume wa Mungu - toka Musa mpaka Mtume *s.a.w.* - na umetumiwa katika siku hizi zetu juu ya Seyidna Ahmad, Masihi Aliyeahidiwa na Mwanzilishi wa Mwendeleo wa Ahmadiyya. Maadui zake walimlaumu ya kwamba anawapoteza watu kwa mafundisho ya udanganyifu, na kuleta fitina kati ya Waislamu, wakisahau ya kwamba tokea hapo fitina ilikwisha watafuna Waislamu, na juhudi ya Seyidna Ahmad haikuwa ila kutaka kuunganisha nyuzi zilizokatikakatika za imani.

Aya 83. "Maneno ya Allah" ni "habari njema" na pia ni "maonyo" na ni kwa haya mawili Allah huisimamisha haki. Nabii Musa alieleza ukweli mkubwa katika Aya hii. Anasema ya kwamba Allah hahitaji udanganyifu na uwongo kwa kutangaza dini Yake, bali huizagaza na kuisimamisha kwa kudra na amri Yake isiyobadilika. Maneno haya yana ukweli mkubwa wa mafunzo mema ya kwamba kutangaza jambo zuri hakuhitaji kutumia njia za udanganyifu. Tabia kama ya Paulo asemaye, "Ikiwa kweli ya Mungu imezidi kudhihirisha utukufu wake kwa sababu ya uwongo wangu, mbona mimi ningali nahukumiwa kuwa ni mwenye dhambi?" (Warumi 3:7), haijapata kushikwa na Manabii wa Mungu na wafuasi wao wakweli. Ukweli huenea kwa nguvu uliyo nayo

FUNGU 9

فَمَآ اٰمَنَ لِمُوْسٰٓى اِلَّا ذُرِّيَّةٌ مِّنْ قَوْمِهٖ
عَلٰى خَوْفٍ مِّنْ فِرْعَوْنَ وَمَلَا۟ئِهِمْ اَنْ
يَّفْتِنَهُمْ ؕ وَاِنَّ فِرْعَوْنَ لَعَالٍ فِى الْاَرْضِ ۚ
وَاِنَّهٗ لَمِنَ الْمُسْرِفِيْنَ ﴿٨٣﴾

84. Lakini hawakumwamini Musa isipokuwa baadhi ya wazao wa kaumu yake, kwa sababu ya kumwogopa Firauni na wakuu wao ili wasiwatese. Na hakika Firauni alikuwa mjeuri katika nchi, na kwa yakini alikuwa miongoni mwa wapitao kiasi.

وَقَالَ مُوْسٰى يٰقَوْمِ اِنْ كُنْتُمْ اٰمَنْتُمْ بِاللّٰهِ
فَعَلَيْهِ تَوَكَّلُوْٓا اِنْ كُنْتُمْ مُّسْلِمِيْنَ ﴿٨٤﴾

85. Na Musa akasema: Enyi kaumu yangu! ikiwa ninyi mmemwamini Allah, basi tegemeeni Kwake, kama ninyi mmetii.

فَقَالُوْا عَلَى اللّٰهِ تَوَكَّلْنَا ۚ رَبَّنَا لَا تَجْعَلْنَا
فِتْنَةً لِّلْقَوْمِ الظّٰلِمِيْنَ ﴿٨٥﴾ ۙ

86. Ndipo wakasema: Tunamtegemea Allah. Mola wetu, Usitufanye jaribio kwa watu wadhalimu;

وَنَجِّنَا بِرَحْمَتِكَ مِنَ الْقَوْمِ الْكٰفِرِيْنَ ﴿٨٦﴾

87. Na Utuokoe kwa rehema Yako katika watu makafiri.

وَاَوْحَيْنَآ اِلٰى مُوْسٰى وَاَخِيْهِ اَنْ تَبَوَّاٰ
لِقَوْمِكُمَا بِمِصْرَ بُيُوْتًا وَّاجْعَلُوْا

88. Na Tulimfunulia Musa na nduguye ya kwamba: Jengeni majumba kwa ajili ya watu wenu katika mji. Na

Aya 85. Maneno haya, *Kama ninyi mmetii,* yakitanguliwa na maneno, *Ikiwa ninyi mmemwamini Allah*, si kama yamezidishwa tu bila kuwepo haja, bali yametumiwa kueleza wazo jingine. Neno *Islaam* (utii) linapotumiwa pamoja na neno *Iimaan* (imani), basi hili la nyuma maana yake huwa uaminifu na imani madhubuti, ambapo la kwanza linaonyesha utii wa nje wa kutii mamlaka. Ndio kusema, *Iimaan* linaonyesha "utii wa moyo," ambapo *Islaam* linaonyesha "utii wa nje wa matendo." Katika jiha hii Aya hii italeta maana ya kwamba, "Kama mmepata imani juu ya Allah na sasa mnataka kuonja matunda ya imani hiyo kwa matendo, basi mtegemeeni Mungu na mmwakilishe mambo yenu yote."

Aya hii inatufundisha ya kwamba imani ya ndani lazima ifuatwe na mabadiliko halisi ya nje katika maisha ya mtu. Kwa mumini wa kweli, *Iimaan* huja kwanza na *Islaam* hufuata nyuma. Lakini kwa hao walio na imani dhaifu, *Islaam* huitangulia *Iimaan,* kwa maana udhaifu wa imani awali huanza pamoja na maonyesho ya nje ya kutii, na pole pole mtu anapata imara ya moyo. Hivyo kwa mumini wa kweli, usafi wa moyo, huutangulia usafi wa matendo. Lakini kinyume na hivi ndio hali ya wenye imani dhaifu, maana mtu wa namna hiyo anahitaji kupata msaada utokao nje ili kuusafisha moyo wake. Kwa hiyo usafi wa vitendo vyake unautangulia usafi wa moyo wake. Ni kwa sababu hii Qur'an inawaambia mabedui: *Sema: Hamjaamini, lakini semeni: Tumesilimu: maana imani haijaingia mioyoni mwenu* (sura 49:15).

Aya 88. Neno *Qibla* katika maana ya *Mutaqaabila* lina maana ya kukabiliana au kuelekeana. Pia lina maana ya upande, namnaau jinsi (Akrab na Lane). Kadhalika lina maana ya upande anaoelekea mtu wakati wa kusali; kitu chochote anachokielekea; na pia Kaaba tunayoielekea wakati wa kusali (Akrab).

mzifanye nyumba zenu zikabiliane, na simamisheni Sala. Na uwape habari njema waaminio.

بُيُوْتَكُمْ قِبْلَةً وَّاَقِيْمُوا الصَّلٰوةَ ؕ وَبَشِّرِ الْمُؤْمِنِيْنَ ﴿٨٨﴾

89. Na Musa akasema: Mola wetu, bila shaka Umempa Firauni na wakuu wake mapambo na mali nyingi katika maisha ya dunia, je ee Mola wetu, ili wawapoteze (watu) katika njia Yako? Mola wetu ziangamize mali zao na iadhibu mioyo yao, maana hawataamini mpaka waione adhabu iumizayo.

وَقَالَ مُوْسٰى رَبَّنَآ اِنَّكَ اٰتَيْتَ فِرْعَوْنَ وَمَلَاَهٗ زِيْنَةً وَّاَمْوَالًا فِى الْحَيٰوةِ الدُّنْيَا ۙ رَبَّنَا لِيُضِلُّوْا عَنْ سَبِيْلِكَ ۚ رَبَّنَا اطْمِسْ عَلٰٓى اَمْوَالِهِمْ وَاشْدُدْ عَلٰى قُلُوْبِهِمْ فَلَا يُؤْمِنُوْا حَتّٰى يَرَوُا الْعَذَابَ الْاَلِيْمَ ﴿٨٩﴾

90. (Allah) Akasema: Maombi yenu yamekubaliwa, basi kuweni imara, wala msifuate njia ya wale wasiojua.

قَالَ قَدْ اُجِيْبَتْ دَّعْوَتُكُمَا فَاسْتَقِيْمَا وَلَا تَتَّبِعٰٓنِّ سَبِيْلَ الَّذِيْنَ لَا يَعْلَمُوْنَ ﴿٨٩﴾

91. Na Tukawapitisha wana wa Israeli katika bahari; lakini Firauni na majeshi yake wakawafuata kwa uasi na dhulma. Hata ilipomfikia gharika, akasema: Naamini ya kwamba hakuna aabudiwaye ila Yule wanayemwamini wana wa Israeli, na mimi ni miongoni mwa wanaotii.

وَجٰوَزْنَا بِبَنِىْٓ اِسْرَآءِيْلَ الْبَحْرَ فَاَتْبَعَهُمْ فِرْعَوْنُ وَجُنُوْدُهٗ بَغْيًا وَّعَدْوًا ؕ حَتّٰٓى اِذَآ اَدْرَكَهُ الْغَرَقُ ۙ قَالَ اٰمَنْتُ اَنَّهٗ لَآ اِلٰهَ اِلَّا الَّذِىْٓ اٰمَنَتْ بِهٖ بَنُوْٓا اِسْرَآءِيْلَ وَاَنَا مِنَ الْمُسْلِمِيْنَ ﴿٩١﴾

Amri waliyopewa ya kukaa mjini, sio maana yake kuwa kabla ya amri hii, Waisraeli walikuwa wakiishi porini. bali Aya inatilia mkazo kwamba maisha ya kistaarabu na ya umoja ni ya lazima na yenye manufaa.

Kwa kuangalia maana mbali mbali za neno "Qibla," maneno ya Kurani, *Kuzifanya nyumba zenu zikabiliane;* yanaweza kuwa na maana hizi:- (1) Waisraeli waliambiwa kukaa pamoja ili waweze kusaidiana katika nyakati za haja, maana watu huweza kusaidiana wanapokuwa wamejenga nyumba zao karibu karibu, au zikikabiliana; au (2) ya kwamba Waisraeli wafanye nyumba zao zielekee upande mmoja, jambo ambalo, kwa undani, linaashiria ya kuwa waungane kindugu na wawe na kusudio au shabaha moja; au (3) kwamba nyumba zao zote ziwe namna moja, ikidokezwa ya kwamba kuwe na undugu wa hakika kati ya tajiri na masikini na wote washughulike pamoja katika hali ya kufanana; kwa sababu hakuwezi kuwa na ujamaa wenye nguvu wanapokuwa baadhi yao wanaishi katika majumba ya fahari ya kisultani na wengine katika vibuguru vibovu.

Kwa neno zima, Aya hii imeweka kanuni saba zifuatazo zenye hekima ambazo kwa kuzifuata watu watainuka na kustawi: (1) Waishi pamoja; (2) wawe na umoja; (3) wasaidiane sana; (4) wawe na usikizi na taratibu; (5) wasibaguane watu wa hali mbalimbali; (6) waombe msaada wa Allah daima kwa maombi ya unyenyekevu na (7) wawe wavumilivu. Mwisho, Aya hii imetoa maagizo yenye maana sana kwa ajili ya Mkuu au Kiongozi wa watu, ya kwamba aendelee kutoa "habari njema", yaani awaambie maneno ya kuwatia nguvu na kuwapa moyo watu wake, kwani kitu kinachoharibu mafanikio ni kukata tamaa na kufa moyo.

Aya 89. Katika dua hii, *Mola wetu, ziangamize mali zao na ishambulie mioyo yao*, Nabii

92. Je! Sasa (ndio unaamini)! hali uliasi zamani na ulikuwa miongoni mwa waharibifu.

آٰلْـٰٔنَ وَقَدْ عَصَيْتَ قَبْلُ وَكُنْتَ مِنَ الْمُفْسِدِيْنَ ﴿٩٢﴾

93. Basi leo Tutakuokoa kwa (kuuweka) mwili wako ili uwe Ishara kwa ajili ya wa nyuma yako. Na kwa kweli watu wengi wameghafilika na Ishara Zetu.

فَالْيَوْمَ نُنَجِّيْكَ بِبَدَنِكَ لِتَكُوْنَ لِمَنْ خَلْفَكَ اٰيَةً ؕ وَاِنَّ كَثِيْرًا مِّنَ النَّاسِ عَنْ اٰيٰتِنَا لَغٰفِلُوْنَ ﴿٩٣﴾ ع

Musa hamtakii Firauni na watu wake ubaya, bali dua hiyo ni kwa ajili ya kuwatakia heri. Aliona ya kwamba wamekuwa wagumu sana katika kufuru yao hata hakuna kitu kingeweza kuwafanya waamini isipokuwa adhabu kali ya Allah. Hivyo Nabii Musa aliomba wateremshiwe adhabu, si ya kuwahilikisha, bali mioyo yao ishambuliwe na igeukie kwenye haki. Hivyo dua hiyo inaonekana kama ya kutaka Firauni na mawaziri wake waangamie, lakini hakika yake ni dua ya kuwatakia waongoke. Dua hii inafanana na mtu anayemhurumia mwenziwe mwenye kiungo kinachooza akimwombea kikatwe ili kisiwe sababu ya kumwua. Hivyo hakuna shaka dua hii ni ya kuwatakia heri ingawa inaonekana katika maneno makali.

Aya 92. Maneno haya ya ufasaha *Je! Sasa!* yanaonyesha ya kwamba imani inayoweza kumfaa mtu ni ile anayoamini katika wakati uliowekwa ili aamini. Lakini haki inapokuwa wazi kabisa na hakukubakia shaka wala matatanisho hata kidogo, imani hapo haina thamani. Kwa hakika ni juhudi na kujitoa sadaka vinavyomfanya mtu astahili thawabu, na hivi viwili vinapokosekana basi mtu anapoteza haki zote za kupata thawabu.

Aya 93. Ujira unaotolewa na Allah kwa hakika huwa na maana ya undani sana. Firauni aliamini wakati ambao imani yake haikuwa cho chote zaidi kuliko kiwiliwili kisicho na roho; hivyo Allah naye akaponyesha kiwiliwili chake tu, na roho yake isipewe nafasi ya kufaidika kwa imani ile. Kiwiliwili chake kiliponyeshwa ili kiwe fundisho kwa ajili ya karne zitakazofuata.

Ni wazi ya kuwa Qur'an peke yake ndio inayotaja jambo hili. Biblia haitaji habari hii ya kupona kiwiliwili cha Firauni, wala hakuna kitabu cho chote cha historia kinachotaja habari hii. Lakini ni kwa namna ya ajabu iliyoje neno hili la Allah lilivyohakiki kuwa la kweli! Baada ya kupita zaidi ya miaka 3,000, kiwiliwili cha Firauni kimegunduliwa, na sasa kiko katika hali ya kuhifadhiwa katika makumbusho ya Cairo, mji mkuu wa Misri. Mwili huo unaonyesha Firauni alikuwa mtu mwembamba, mfupi, mwenye wajihi unaoonyesha hasira na upumbavu. Angalieni wakati wetu huu uko mbali kadiri gani na wakati alioishi Firauni; lakini Mungu Mwenye uwezo si kama aliusalimisha mwili wake tu, bali ameuhifadhi mpaka hivi leo.

Aya hii inatoa stishihada yenye nguvu sana ya kwamba Qur'an imetoka kwa Mungu na ya kwamba ni Kitabu bora kuliko Biblia ya Wakristo na Mayahudi. Vitabu vitano vya Musa vilivyomo katika Biblia vinadai kueleza historia ya siku za Nabii Musa na inadaiwa ya kwamba vitabu hivyo viliandikwa siku zile zile Nabii Musa angali hai. Lakini Qur'an Iliyokuja miaka ipatayo 2,000 baada ya Taurati imetaja baadhi ya mambo (pamoja na hili) ambayo hayatajwi ndani ya Biblia, lakini matokeo ya baadaye yamehakikisha kuwa ni ya kweli. Jambo hili linasimamisha ukweli wa Qur'an na kutotegemewa kwa Vitabu vya Biblia kwa uwazi kabisa bila shaka yo yote.

Aya hii pia inatoa fundisho kubwa la dini ya kwamba ni lazima tufanye haraka kuikubali haki mara inapotufikia na tusisitesite na kuchelewa, kama alivyofanya Firauni.

Baadhi ya mufasirina wanafikiri ya kuwa Firauni aliyegharikishwa alikuwa Rameses. Lakini

FUNGU 10

وَلَقَدْ بَوَّاْنَا بَنِيٓ اِسْرَآءِيْلَ مُبَوَّاَ صِدْقٍ
وَّرَزَقْنٰهُمْ مِّنَ الطَّيِّبٰتِ ۚ فَمَا اخْتَلَفُوْا
حَتّٰى جَآءَهُمُ الْعِلْمُ ۭ اِنَّ رَبَّكَ يَقْضِيْ
بَيْنَهُمْ يَوْمَ الْقِيٰمَةِ فِيْمَا كَانُوْا فِيْهِ يَخْتَلِفُوْنَ ۝

94. Na bila shaka Tuliwaweka wana wa Israeli makao mazuri, na Tukawaruzuku katika vitu vizuri; nao hawakuhitilafiana mpaka ilipowafikia elimu. Hakika Mola wako Atahukumu kati yao siku ya Kiyama katika yale waliyokuwa wakihitilafiana.

فَاِنْ كُنْتَ فِيْ شَكٍّ مِّمَّآ اَنْزَلْنَآ اِلَيْكَ
فَسْـَٔلِ الَّذِيْنَ يَقْرَءُوْنَ الْكِتٰبَ مِنْ
قَبْلِكَ ۚ لَقَدْ جَآءَكَ الْحَقُّ مِنْ رَّبِّكَ فَلَا
تَكُوْنَنَّ مِنَ الْمُمْتَرِيْنَ ۝

95. Na kama unayo shaka juu ya hayo Tuliyokuteremshia, basi waulize wale wasomao Kitabu kabla yako. Kwa yakini haki imekwisha kukufikia kutoka kwa Mola wako, kwa hiyo usiwe miongoni mwa wafanyao shaka.

---

aliyemlea (Kutoka 1:11), lakini ilikuwa katika utawala wa mwanawe aitwaye Menfitah (Meneptah) Nabii Musa alipopewa utume (Kutoka 2:23; pia tazama Jew. Enc. vol. viii, pp and Enc. Bib. under *Pharao* and under *Egypt*).

Aya 94. *Ilipowafikia elimu.* Elimu hapa, mradi wake ni Qur'an. Wala si Taurati maana hapakupita muda baina ya kushuka Taurati na kujiweka Waisraeli katika umoja. Hivyo hawawezi kusemwa walihitilafiana baada ya kushuka Taurati.

Ilipokuwa karibu kudhihiri Mtume Muhammad *s.a.w.* Mayahudi walikuwa wakisadiki ya kwamba Mtume anayefanana na Musa alikuwa karibu kutokea; lakini Mtume aliyeahidiwa alipotokea hasa, wakahitilafiana juu ya kusema ni nani hasa aliyehusika na bishara zile. Baadhi ya Mayahudi walikataa kusadiki kuwa bishara zile zimetimia katika dhati ya Mtume Muhammad *s.a.w.* na wengine wakatafuta kukataa kuwapo kwa bishara za namna hiyo.

Kusema kwamba kutopatana kunakotajwa ndani ya Aya hii kunawahusu Waisraeli baada ya kushuka Qur'an, kunadhihirika pia katika Aya ifuatayo inayosema, Na (ewe msikiaji) *kama unayo shaka juu ya hayo Tuliyokuteremshia* (yaani Qur'an). Aya ya pili ya hii inaonyesha waziwazi ya kuwa "elimu" inayotajwa katika Aya hii, ambayo baada ya kufika Waisraeli wakahitilafiana, ni Qur'an.

Mayahudi walikuwa wanangoja kwa shauku sana kudhihiri kwa Nabii aliye kama Musa aliyeahidiwa katika Kumbukumbu 18:18 ambaye walijua atatokea Bara Arabu katika wazao wa Ismail, ndugu za Waisraeli, hata baadhi yao wakahamia Bara Arabu na kukaa Madina ili wawe katika watu wa kwanza kumkubali Mtume huyo atakapotokea. Kwa hakika ni kinyume cha mambo kuona ya kwamba wale wale waliomngojea kwa shauku wakawa ndio maadui wake wakubwa.

Aya 95. *Na kama unayo shaka juu ya hayo Tuliyokuteremshia.* Maneno haya haambiwi Mtume *s.a.w.* wala masahaba wake, bali wanaambiwa wale waliohitilafiana baada ya kuwafikia elimu ya Qur'an ambao wametajwa katika Aya 94 hapo juu.

96. Wala usiwe miongoni mwa wale wanaokadhibisha Ishara za Allah, usije ukawa miongoni mwa wenye hasara.

وَلَا تَكُوْنَنَّ مِنَ الَّذِيْنَ كَذَّبُوْا بِاٰيٰتِ اللّٰهِ فَتَكُوْنَ مِنَ الْخٰسِرِيْنَ ﴿٩٥﴾

97. Hakika wale ambao neno la Mola wako limekwisha thibitika juu yao, hawataamini

اِنَّ الَّذِيْنَ حَقَّتْ عَلَيْهِمْ كَلِمَتُ رَبِّكَ لَا يُؤْمِنُوْنَ ﴿٩٦﴾

98. Ijapokuwa kila Ishara iwafikie - mpaka waione adhabu iumizayo.

وَلَوْ جَآءَتْهُمْ كُلُّ اٰيَةٍ حَتّٰى يَرَوُا الْعَذَابَ الْاَلِيْمَ ﴿٩٧﴾

99. Basi mbona haukuwako mji ulio-amini na imani yake ikaufaa, isipokuwa watu wa Yunus? Walipoamini Tuliwaon-dolea adhabu ya fedheha katika maisha ya dunia na Tukawafaidisha kwa muda.

فَلَوْلَا كَانَتْ قَرْيَةٌ اٰمَنَتْ فَنَفَعَهَآ اِيْمَانُهَآ اِلَّا قَوْمَ يُوْنُسَ ؕ لَمَّآ اٰمَنُوْا كَشَفْنَا عَنْهُمْ عَذَابَ الْخِزْيِ فِى الْحَيٰوةِ الدُّنْيَا وَمَتَّعْنٰهُمْ اِلٰى حِيْنٍ ﴿٩٨﴾

100. Na kama Angalitaka Mola wako bila shaka wangaliamini wote waliomo katika ardhi pamoja. Basi je, wewe utawashurutisha watu hata wawe waaminio?

وَلَوْ شَآءَ رَبُّكَ لَاٰمَنَ مَنْ فِى الْاَرْضِ كُلُّهُمْ جَمِيْعًا ؕ اَفَاَنْتَ تُكْرِهُ النَّاسَ حَتّٰى يَكُوْنُوْا مُؤْمِنِيْنَ ﴿٩٩﴾

Aya 97. Aya hii inaonyesha ya kuwa watu wanaokuwa wamestahili adhabu na hawakufanya juhudi yo yote kuiepuka, ingawa wameonywa, hao hawataamini.

Aya 99. Yunus ni jina la Nabii aliyeishi katika karne ya 9 kabla ya Nabii Isa. Hapa hali ya Nabii *s.a.w.* inaonyeshwa kuwa imefanana sana na Nabii Yunus. Watu wa Ninawi mwanzoni walimpinga kabisa Nabii Yunus, naye akawabashiria kuwa punde wataadhibiwa. Baadaye walipoona adhabu inakaribia, wakatubu. Kadhalika watu wa Makka waliomkataa Mtume, Makka iliposhindwa na Waislamu, nao wakaingia Uislamu, na kwa njia hii wakaipona adhabu ya Allah.

Aya 100. Maneno haya, *Basi je, wewe utawashurutisha watu hata wawe waaminio?* yanaweza kufasiriwa namna mbili: (1) yanaweza kuchukuliwa kama hoja iliyotolewa kutia nguvu maneno yaliyosemwa katika sehemu ya kwanza ya Aya hii hii. Hivyo maana yake itakuwa ya kwamba Allah hataki kumshurutisha mtu katika habari za dini, maana kumshurutisha mtu kufuata dini fulani hakuwezi kuleta manufaa yo yote. Hivyo Qur'an inamwuliza Mtume kama angependa kuwashurutisha watu wafuate Dini yake bila wenyewe kupenda, ikiweka shabaha ya jibu la kukana maana Mtume hangependelea kamwe kutumia nguvu Aya inatangaza ya kwamba Allah ambaye anajua siri za mioyo yote, hawezi kutumia karaha.

(2) Aya hii pia inaweza kuchukuliwa kwamba maneno hayo anaambiwa kila mumini ya kuwa makafiri kukataa haki si jambo la kumtia hasira mtu ye yote na kumfanya awashurutishe kuikubali; na hoja inayotolewa ni kwamba Allah ndiye Mola na Bwana wa viumbe

وَمَا كَانَ لِنَفْسٍ اَنْ تُؤْمِنَ اِلَّا بِاِذْنِ اللّٰهِ ؕ وَيَجْعَلُ الرِّجْسَ عَلَى الَّذِيْنَ لَا يَعْقِلُوْنَ ﴿١٠٠﴾

101. Na hakuna mtu awezaye kuamini isipokuwa kwa idhini ya Allah. Naye Huweka hasira juu ya wale ambao hawatumii akili.

قُلِ انْظُرُوْا مَاذَا فِى السَّمٰوٰتِ وَالْاَرْضِ ؕ وَمَا تُغْنِى الْاٰيٰتُ وَالنُّذُرُ عَنْ قَوْمٍ لَّا يُؤْمِنُوْنَ ﴿١٠١﴾

102. Sema: Tazameni ni nini yanayotokea katika mbingu na ardhi! na ishara na waonyaji haviwafai watu wasioamini.

فَهَلْ يَنْتَظِرُوْنَ اِلَّا مِثْلَ اَيَّامِ الَّذِيْنَ خَلَوْا مِنْ قَبْلِهِمْ ؕ قُلْ فَانْتَظِرُوْۤا اِنِّىْ مَعَكُمْ مِّنَ الْمُنْتَظِرِيْنَ ﴿١٠٢﴾

103. Nao hawangoji ila mfano wa siku za watu waliopita kabla yao. Sema: Basi ngojeni, mimi pia ni pamoja nanyi katika wangojeao.

ثُمَّ نُنَجِّىْ رُسُلَنَا وَالَّذِيْنَ اٰمَنُوْا كَذٰلِكَ ۚ حَقًّا عَلَيْنَا نُنْجِ الْمُؤْمِنِيْنَ ﴿١٠٣﴾

104. Ndipo Tutawaokoa Mitume Wetu na wale walioamini. Ndivyo ilivyo haki juu Yetu kuwaokoa waaminio.

FUNGU 11

قُلْ يٰۤاَيُّهَا النَّاسُ اِنْ كُنْتُمْ فِىْ شَكٍّ مِّنْ دِيْنِىْ فَلَاۤ اَعْبُدُ الَّذِيْنَ تَعْبُدُوْنَ مِنْ دُوْنِ اللّٰهِ وَلٰكِنْ اَعْبُدُ اللّٰهَ الَّذِىْ يَتَوَفّٰىكُمْ ۖ وَاُمِرْتُ اَنْ اَكُوْنَ مِنَ الْمُؤْمِنِيْنَ ﴿١٠٤﴾

105. Sema: Enyi watu! ikiwa ninyi mnayo shaka katika dini yangu, basi mimi siwaabudu wale mnaowaabudu badala ya Allah, bali namwabudu Allah Ambaye Huwafisheni; na nimeamrishwa niwe miongoni mwa waaminio;

وَاَنْ اَقِمْ وَجْهَكَ لِلدِّيْنِ حَنِيْفًا ۚ وَلَا تَكُوْنَنَّ مِنَ الْمُشْرِكِيْنَ ﴿١٠٥﴾

106. Na kwamba: Elekeza uso wako kwenye dini kwa nia safi, wala usiwe miongoni mwa washirikina.

---

vyote, juu ya hayo hatumii nguvu, basi mtu ye yote hana haki ya kutumia nguvu. Tafsiri ye yote katika hizi mbili inaonyesha waziwazi ya kuwa dini ya Kiislamu hairuhusu kuieneza kwa kutumia nguvu.

وَلَا تَدْعُ مِنْ دُوْنِ اللّٰهِ مَا لَا يَنْفَعُكَ وَلَا يَضُرُّكَ ۚ فَاِنْ فَعَلْتَ فَاِنَّكَ اِذًا مِّنَ الظّٰلِمِيْنَ ﴿١٠٧﴾

107. Wala usiite kinyume na Allah cho chote kisichokufaa wala kisichokudhuru; na ukifanya, basi hakika utakuwa miongoni mwa wadhalimu.

وَاِنْ يَّمْسَسْكَ اللّٰهُ بِضُرٍّ فَلَا كَاشِفَ لَهٗۤ اِلَّا هُوَ ۚ وَاِنْ يُّرِدْكَ بِخَيْرٍ فَلَا رَآدَّ لِفَضْلِهٖ ؕ يُصِيْبُ بِهٖ مَنْ يَّشَآءُ مِنْ عِبَادِهٖ ؕ وَهُوَ الْغَفُوْرُ الرَّحِيْمُ ﴿١٠٨﴾

108. Na kama Allah Akugusishe dhara, basi hakuna ye yote awezaye kuiondoa isipokuwa Yeye; na kama Akutakie heri, basi hakuna awezaye kuzuia fadhili Zake. Huzifikisha (fadhili) kwa Amtakaye katika watu Wake, naye ndiye Msamehevu, Mrehemevu.

قُلْ يٰۤاَيُّهَا النَّاسُ قَدْ جَآءَكُمُ الْحَقُّ مِنْ رَّبِّكُمْ ۚ فَمَنِ اهْتَدٰى فَاِنَّمَا يَهْتَدِيْ لِنَفْسِهٖ ۚ وَمَنْ ضَلَّ فَاِنَّمَا يَضِلُّ عَلَيْهَا ۚ وَمَاۤ اَنَا عَلَيْكُمْ بِوَكِيْلٍ ﴿١٠٩﴾

109. Sema: Enyi watu! haki imekwisha wafikieni kutoka kwa Mola wenu; basi anayeongoka, anaongoka kwa faida ya nafsi yake; na anayepotea, basi anapotea kwa hasara ya nafsi yake; na mimi si mchungaji juu yenu.

وَاتَّبِعْ مَا يُوْحٰۤى اِلَيْكَ وَاصْبِرْ حَتّٰى يَحْكُمَ اللّٰهُ ۚ وَهُوَ خَيْرُ الْحٰكِمِيْنَ ﴿١١٠﴾ ع

110. Na ufuate yanayofunuliwa kwako, na usubiri mpaka Allah Atoe hukumu. Naye ndiye Mbora wa mahakimu.

Aya 107. *Wala usiite kinyume na Allah cho chote kisichokufaa wala kisichokudhuru,* siyo maana ya maneno haya kuwa tunaweza kuviita kinyume na Allah vitu vinavyotufaa na kutudhuru. Maana yake ni kuwa cho chote kisichokuwa Allah hakina uwezo wa kujitegemea wa kutunufaisha wala wa kutudhuru; hivyo tusitegemee cho chote isipokuwa Allah. Neno *Adh-Dhaalimiin* (wadhalimu) hapa limetumiwa kwa maana ya *mushrikiin,* yaani watu wanaomshirikisha Allah na miungu wengine kwa namna yo yote. Maana hii inatiwa nguvu na hadithi ya Mtume s.a.w isemayo kwamba *dhulm* ni namna ya *shirk* (Bukhari sura *Tafsiir*).

Aya 110. *Yeye ndiye Mbora wa mahakimu.* Maneno haya yanaonyesha ya kuwa hukumu ya Allah itakuwa bora kwa ajili ya Mtume wake. Nasi tunaona ya kuwa hukumu ile ilipofika, dunia ikashtukiziwa. Wale waliokuwa na kiu ya damu ya Mtume *s.a.w.* wakawa wafuasi wake wanyenyekevu kabisa, na nchi nzima ya Bara Arabu, kama vile watu wa Yunus, wakamwamini; na makabila ya kila upande yakamjia upesi upesi kumtii.

سُوْرَةُ هُوْدٍ مَّكِّيَّةٌ وَّ هِيَ مَعَ الْبَسْمَلَةِ مِائَةٌ وَّ اَرْبَعٌ وَّ عِشْرُوْنَ اٰيَةً وَّ عَشَرَةُ رُكُوْعَاتٍ

11. SURA HUUD

Imeteremshwa Makka

Ina mafungu 10 na Aya 124 pamoja na Bismillahi

بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ ①

1. Kwa jina la Allah, Mwingi wa rehema, Mwingi wa ukarimu.

الٓرٰ ۟ كِتٰبٌ اُحْكِمَتْ اٰيٰتُهٗ ثُمَّ فُصِّلَتْ مِنْ لَّدُنْ حَكِيْمٍ خَبِيْرٍ ۙ ②

2. Mimi ni Allah Nionaye. Hiki ni Kitabu ambacho Aya zake zinalindwa kisha zimeelezwa kinaganaga na Mwenye hekima, Mwenye habari.

اَلَّا تَعْبُدُوْٓا اِلَّا اللّٰهَ ؕ اِنَّنِيْ لَكُمْ مِّنْهُ نَذِيْرٌ وَّ بَشِيْرٌ ۙ ③

3. Kwamba msiabudu isipokuwa Allah. Hakika mimi nimetoka Kwake kuwa Mwonyaji na Mtoaji wa habari njema kwenu.

وَّ اَنِ اسْتَغْفِرُوْا رَبَّكُمْ ثُمَّ تُوْبُوْٓا اِلَيْهِ يُمَتِّعْكُمْ مَّتَاعًا حَسَنًا اِلٰٓى اَجَلٍ مُّسَمًّى وَّ يُؤْتِ كُلَّ ذِيْ فَضْلٍ فَضْلَهٗ ؕ وَ اِنْ تَوَلَّوْا فَاِنِّيْٓ اَخَافُ عَلَيْكُمْ عَذَابَ يَوْمٍ كَبِيْرٍ ④

4. Na ya kwamba mwombe msamaha kwa Mola wenu, kisha mtubie Kwake. Atawafaidisheni kwa manufaa mazuri mpaka muda maalum, na Atampa kila mwenye fadhili, fadhili yake. Na kama mtageuka, basi nawahofieni adhabu ya siku kubwa.

Hii ni sura ya Makka. Ibni Abbas, Al-Hassan, Ikrama, Mujahid, Katada na Jabir bin Zaid wanasema ya kuwa sura hii yote ilishuka Makka. Lakini katika hadithi nyingine Ibni Abbas anaibagua Aya 13 na kusema ya kuwa ilishuka Madina. Na Mukatil anasimulia ya kuwa sura yote ilishuka Makka, isipokuwa Aya 13, 18 na 115.

Aya 2. *Uhkimat aayaatuhuu,* "Aya zake zimelindwa." Mradi ni kwamba Aya za Qur'an zimefanywa kuwa nzima na imara kwa hoja na dalili; au zimehifadhiwa zisipate kuharibiwa; au zina hekima; au mafundisho ya Kitabu hiki yanamzuia mtu katika maovu.

Aya 3. Ibada, mradi wake ni kuziangalia daima sifa za Allah na kuzisimika akili, na kwa kufanya hivi tunajifaidisha sisi wenyewe na hatumfanyii Mungu wema wo wote. Kuna hadithi ya Mtume s.a.w. inayokubali maelezo hayo. Alipoulizwa ibada ni nini, akajibu, "Umwabudu Mungu kama unayemwona," yaani sifa mbali mbali za Allah mtu aziweke mbele yake na kuzifikiria (Bukhari, sura ya *Imraan*).

Aya 4. *Mwombe msamaha kwa Mola wenu.* Neno la Kiarabu lililotumika kwa kuomba msamaha ni *Istighfaar* (kuomba ghofira) ambalo maana yake hasa ni "kumwomba Mungu afunike."

5. Marejeo yenu ni kwa Allah; naye ni Mwenye uwezo juu ya kila kitu.

إِلَى اللّٰهِ مَرْجِعُكُمْ ۚ وَهُوَ عَلٰى كُلِّ شَىْءٍ قَدِيرٌ ۝٥

6. Sikilizeni! bila shaka wao wanakunja vifua vyao ili wajifiche naye. Sikilizeni, wanapozivaa nguo zao, Anajua wanayoyaficha na wanayoyadhihirisha. Hakika Yeye ni Mjuzi wa yaliyomo vifuani.

أَلَآ إِنَّهُمْ يَثْنُونَ صُدُورَهُمْ لِيَسْتَخْفُوا۟ مِنْهُ ۚ أَلَا حِينَ يَسْتَغْشُونَ ثِيَابَهُمْ ۙ يَعْلَمُ مَا يُسِرُّونَ وَمَا يُعْلِنُونَ ۚ إِنَّهُۥ عَلِيمٌۢ بِذَاتِ ٱلصُّدُورِ ۝٦

JUZU 12

7. Na hakuna mnyama ye yote katika ardhi isipokuwa riziki yake iko juu ya Allah. Na Anayajua makao yake ya kudumu na makao yake ya muda. Yote yamo katika Kitabu dhahiri.

وَمَا مِن دَآبَّةٍ فِى ٱلْأَرْضِ إِلَّا عَلَى ٱللّٰهِ رِزْقُهَا وَيَعْلَمُ مُسْتَقَرَّهَا وَمُسْتَوْدَعَهَا ۚ كُلٌّ فِى كِتَٰبٍ مُّبِينٍ ۝٧

8. Na Yeye ndiye Aliyeziumba mbingu na ardhi katika nyakati sita, na Enzi Yake iko juu ya maji, ili kuwajaribuni ni nani miongoni mwenu mwenye vitendo bora. Na kama ukisema, Bila shaka ninyi mtafufuliwa baada ya kufa, kwa yakini wale waliokufuru watasema: Siyo haya ila ni udanganyifu waziwazi.

وَهُوَ ٱلَّذِى خَلَقَ ٱلسَّمَٰوَٰتِ وَٱلْأَرْضَ فِى سِتَّةِ أَيَّامٍ وَكَانَ عَرْشُهُۥ عَلَى ٱلْمَآءِ لِيَبْلُوَكُمْ أَيُّكُمْ أَحْسَنُ عَمَلًا ۗ وَلَئِن قُلْتَ إِنَّكُم مَّبْعُوثُونَ مِنۢ بَعْدِ ٱلْمَوْتِ لَيَقُولَنَّ ٱلَّذِينَ كَفَرُوٓا۟ إِنْ هَٰذَآ إِلَّا سِحْرٌ مُّبِينٌ ۝٨

Kwa maana hii mradi wake itakuwa ya kwamba tumwombe Mungu siku zote afunike maelekeo yetu ya uovu na matamanio yanayotuzuia katika kumkaribia.

Kisha mtubie Kwake. Hao wanaodhani ya kuwa fundisho la Kiislamu la toba linahimiza mtu kufanya dhambi, hawajui kabisa mradi wake. Kwa hakika ni upumbavu kudhania mtu anayefanya bidiii kuondoa matokeo mabaya ya dhambi zake na kuyavunja matamanio yake mabaya ya kwamba ni maneno ya mdomo tu. Kwa hakika toba ni tendo la kuelekea kwa Allah kwa moyo wote baada ya kumwomba akulinde na matokeo mabaya ya dhambi zilizopita. Je, kuna njia bora zaidi kuliko hii ya kutaka kumkaribia Allah?

Aya 7. Qur'an inaeleza katika Aya hii ya kuwa Allah ambaye huwatimizia hata wanyama na wadudu riziki zao na mahitaji yao yote asingeweza kumwacha mwanadamu, ambaye ndiye mbora wa viumbe vyote, bila kumtimizia haja zake za kimwili na za kiroho. Hivyo ni juu ya mwanadamu mwenyewe kujifaidisha na neema hizo alizowekewa.

Aya 8. *Enzi Yake iko juu ya maji.* Qur'an imeeleza mara kwa mara kuwa chanzo cha uhai

وَلَئِنْ اَخَّرْنَا عَنْهُمُ الْعَذَابَ اِلٰٓى اُمَّةٍ
مَّعْدُوْدَةٍ لَّيَقُوْلُنَّ مَا يَحْبِسُهٗ ؕ اَلَا يَوْمَ
يَاْتِيْهِمْ لَيْسَ مَصْرُوْفًا عَنْهُمْ وَحَاقَ
بِهِمْ مَّا كَانُوْا بِهٖ يَسْتَهْزِءُوْنَ ۝٩ ع

9. Na kama Tukiwakawizia adhabu mpaka muda uliohesabiwa, bila shaka watasema: Ni nini kinachoizuia? Sikilizeni! siku itakapowafikia haitaondolewa kwao, na yatawazunguka yale waliyokuwa wakiyafanyia mzaha.

FUNGU 2

وَلَئِنْ اَذَقْنَا الْاِنْسَانَ مِنَّا رَحْمَةً ثُمَّ نَزَعْنٰهَا
مِنْهُ ۚ اِنَّهٗ لَيَـُٔوْسٌ كَفُوْرٌ ۝١٠

10. Na kama Tukimwonjesha mwanadamu rehema kutoka Kwetu, kisha Tukaiondoa kwake, bila shaka yeye anakuwa mwenye kukata tamaa kabisa, asiye shukurani.

وَلَئِنْ اَذَقْنٰهُ نَعْمَآءَ بَعْدَ ضَرَّآءَ مَسَّتْهُ
لَيَقُوْلَنَّ ذَهَبَ السَّيِّاٰتُ عَنِّىْ ؕ اِنَّهٗ
لَفَرِحٌ فَخُوْرٌ ۝١١ۙ

11. Na kama Tukimwonjesha neema baada ya dhara iliyompata, bila shaka husema, Taabu zote zimeniondoka. Kwa hakika yeye ndiye mwenye kufurahi sana, mwenye kujivuna sana.

اِلَّا الَّذِيْنَ صَبَرُوْا وَعَمِلُوا الصّٰلِحٰتِ ؕ
اُولٰٓئِكَ لَهُمْ مَّغْفِرَةٌ وَّاَجْرٌ كَبِيْرٌ ۝١٢

12. Isipokuwa wale wanaosubiri na kufanya vitendo vizuri, hao ndio wapatao msamaha na ujira mkubwa.

فَلَعَلَّكَ تَارِكٌ بَعْضَ مَا يُوْحٰٓى اِلَيْكَ
وَضَآئِقٌ بِهٖ صَدْرُكَ اَنْ يَّقُوْلُوْا لَوْلَآ
اُنْزِلَ عَلَيْهِ كَنْزٌ اَوْ جَآءَ مَعَهٗ مَلَكٌ ؕ
اِنَّمَآ اَنْتَ نَذِيْرٌ ؕ وَاللّٰهُ عَلٰى كُلِّ شَىْءٍ
وَّكِيْلٌ ۝١٣ؕ

13. Basi huenda utaacha baadhi ya yale yaliyofunuliwa kwako, na kifua chako kuona dhiki kwayo kwa sababu wanasema: Mbona hakuteremshiwa hazina au kuja Malaika pamoja naye? Wewe ni Mwonyaji tu, na Allah ndiye Mwangalizi wa kila kitu.

---

zinazomiliki na kuendesha ulimwengu. Hivyo, mradi wa maneno hayo ni kwamba sifa za Allah zimedhihirika katika "uhai" (yaani viumbe vilivyo hai) na hasa mwanadamu ambaye ni mkubwa wa viumbe vyote. Kadhalika, *Enzi Yake iko juu ya maji,* ni maneno yanayoweza kuwa na maana ya kwamba ufunuo wa Allah mara kwa mara umefananishwa na maji. Basi ndiyo kusema, sifa za Allah kwa kudhihirishwa kwao zinategemea neno la Mungu analowafunulia watu.

Aya 13. *Basi huenda utaacha*. Neno *la'alla* limetumiwa kuonyesha: "Watu wanaodhani ya kuwa labda sasa utaacha baadhi ya yale yaliyofunuliwa kwako n.k.w." (Mufradat).

14. Je, wanasema, Amekitunga? Sema: Basi leteni sura kumi zilizotungwa mfano wa hii, na waiteni mwezao badala ya Allah ikiwa mu wakweli.

اَمۡ يَقُوۡلُوۡنَ افۡتَرٰىهُ ؕ قُلۡ فَاۡتُوۡا بِعَشۡرِ سُوَرٍ مِّثۡلِهٖ مُفۡتَرَيٰتٍ وَّ ادۡعُوۡا مَنِ اسۡتَطَعۡتُمۡ مِّنۡ دُوۡنِ اللّٰهِ اِنۡ كُنۡتُمۡ صٰدِقِيۡنَ ﴿۱۴﴾

Baadhi ya maadui wa Uislamu wanatafuta kutoa ibara katika Aya hii ya kuwa Mtume *s.a.w.* alikuwa tayari kuacha baadhi ya maneno ya Qur'an kwa sababu ya ubishi wa wapinzani wake. Lakini maneno yenyewe yanabatilisha tafsiri hii ya ovyo. Je, kuna mtu ye yote mwenye akili anayeweza kudhani ya kwamba kwa sababu makafiri walimwambia Mtume hashukiwi na Malaika wa kumsaidia na hateremshiwi hazina, basi Mtume aone inafaa aache baadhi ya maneno aliyofunuliwa na Allah? Au je, kuna mtu mwenye akili anayeweza kudhani ya kuwa Mtume *s.a.w* alikuwa hana habari kuwa yeye ni Mwonyaji tu aliyetumwa kufikisha ujumbe na uwe wa namna gani? Je, Mtume hakujua kwamba Allah alikwisha mwambia waziwazi ya kuwa Yeye Mwenyewe ndiye "Mlinzi juu ya kila kitu?" Hivyo, maneno haya, *Huenda utaacha baadhi ya yale yaliyofunuliwa kwako,* yanaonyesha tu ya kuwa makafiri walikuwa na tumaini la bure kwa kufikiri huenda Mtume ataacha baadhi ya wahyi alioteremshiwa. Je, hawa waletao upinzani huu hawajui ya kwamba Makureishi walimwendea Mtume na kumwambia aache kulaumu miungu yao au si hivyo watamsaga yeye na watu wa ukoo wake, mara Mtume aliwajibu kuwa hata kama waweke jua mkono wake wa kulia na mwezi mkono wake wa kushoto, hataacha kazi aliyopewa na Allah ya kutangaza dini. Je, mtu ambaye matishio na mabembelezo ya namna mbalimbali hayakumshtusha alipokuwa dhaifu na mnyonge, sasa arukwe na fahamu yote hata awe tayari kuacha baadhi ya maneno aliyoteremshiwa kwa sababu ya ubishi wa kipumbavu?

Aya ya pili ya hii inakadhibisha tafsiri ya watu hao, maana inatoa mashindano ya dunia nzima walete sura kumi zilizo kama sura zozote kumi za Qur'an. Kama Mtume alikuwa na shaka yo yote juu ya sehemu fulani ya Qur'an, je ingewezekana kutoa mashindano ya aina hii? Mashindano haya yanaonyesha ya kuwa alisadiki kila neno la Qur'an kwa imani iliyo imara kama mwamba.

Aya 14. Aya hii inahakikisha tafsiri ya Aya iliyotangulia. Aya hii ilitoa majibu mawili kwa ajili ya matazamio ya ovyo ya makafiri ya kwamba huenda Mtume *s.a.w.* ataacha baadhi ya maneno ya Qur'an kwa kuogopa upinzani wao. Jibu la kwanza ni kuwa Mtume *s.a.w* ni Mwonyaji tu; hakudai kuwa yeye ni mungu hata atakiwe kuwa na hazina na Malaika; (2) Ya kwamba yeye ni Mjumbe tu aliyeleta ujumbe utokao kwa Allah, na kazi yake ilikuwa ni kuufikisha tu ujumbe huo kwa watu.

Sasa makafiri wangeweza kumjibu ya kuwa yeye ni mwongo kwa sababu angekuwa ametumwa na Mungu lazima angekuwa na nguvu za namna ya pekee. Aya hii inajibu swali lao hilo, na inasema ya kwamba ingawa Mtume *s.a.w.* hakuwa na hazina za fedha wala dhahabu, bali alikuwa na hazina kubwa kabisa za mambo ya kiroho ambazo watu wa dunia nzima wakusanyike pamoja hawawezi kuwa nazo; na ya kwamba hazina hizo zimo ndani ya Qur'an. Hivyo, kama wao walikanusha kuwa Mtume *s.a.w* si mkweli na kuwa sehemu fulani za ujumbe aliopewa zilikuwa mbaya na zilihitaji kubadilishwa, basi na walete sura zinazofanana na sura hizo kumi wanazoona kuwa ni mbaya. Lakini kwa kuwa hawakuweza kutoa kitabu chenye kulingana na sura hata kumi wanazofikiri ni mbaya, basi lazima wakubali ya kuwa Mtume *s.a.w* anazo hazina za namna ambayo hakuna mwingine anayeweza kuzionyesha. Pia tazama sura 2:24; 10:39; 17:89; na 52:34-35.

15. Na kama wasipowaitikieni, basi jueni ya kwamba kimeteremshwa kwa elimu ya Allah, na ya kwamba hakuna aabudiwaye ila Yeye tu. Basi je, mtakuwa wanyenyekevu?

فَاِلَّمْ يَسْتَجِيْبُوْا لَكُمْ فَاعْلَمُوْٓا اَنَّمَآ
اُنْزِلَ بِعِلْمِ اللّٰهِ وَاَنْ لَّآ اِلٰهَ اِلَّا هُوَ ۚ
فَهَلْ اَنْتُمْ مُّسْلِمُوْنَ ﴿١٤﴾

16. Wanaotaka maisha ya dunia na mapambo yake, Tutawapa humo (ujira wa) vitendo vyao sawasawa, na humo wao hawatapunjwa.

مَنْ كَانَ يُرِيْدُ الْحَيٰوةَ الدُّنْيَا وَزِيْنَتَهَا
نُوَفِّ اِلَيْهِمْ اَعْمَالَهُمْ فِيْهَا وَهُمْ فِيْهَا
لَا يُبْخَسُوْنَ ﴿١٥﴾

17. Hao ndio ambao hawatakuwa na kitu katika Akhera ila Moto, na yataharibika waliyoyafanya katika (dunia) hii, na yatabatilika waliyokuwa wakiyatenda.

اُولٰٓئِكَ الَّذِيْنَ لَيْسَ لَهُمْ فِى الْاٰخِرَةِ اِلَّا
النَّارُ ۖ وَحَبِطَ مَا صَنَعُوْا فِيْهَا وَبٰطِلٌ مَّا
كَانُوْا يَعْمَلُوْنَ ﴿١٦﴾

18. Basi je, (anaweza kuwa mwongo), yule ambaye ana dalili iliyo wazi kutoka kwa Mola wake na shahidi mmoja kutoka Kwake atamfuata, na kabla yake kulikuwa na Kitabu cha Musa kilichokuwa kiongozi na rehema? Hao wanamwamini yeye; na atakayemkataa katika makundi mbalimbali, Moto ndio utakuwa mahali pake pa miadi. Basi usiwe na shaka kuhusu jambo hili. Hakika hii ni haki itokayo kwa Mola wako, lakini watu wengi hawaamini.

اَفَمَنْ كَانَ عَلٰى بَيِّنَةٍ مِّنْ رَّبِّهٖ وَيَتْلُوْهُ
شَاهِدٌ مِّنْهُ وَمِنْ قَبْلِهٖ كِتٰبُ مُوْسٰٓى اِمَامًا
وَّرَحْمَةً ۭ اُولٰٓئِكَ يُؤْمِنُوْنَ بِهٖ ۭ وَمَنْ
يَّكْفُرْ بِهٖ مِنَ الْاَحْزَابِ فَالنَّارُ مَوْعِدُهٗ ۚ
فَلَا تَكُ فِيْ مِرْيَةٍ مِّنْهُ ۣ اِنَّهُ الْحَقُّ مِنْ
رَّبِّكَ وَلٰكِنَّ اَكْثَرَ النَّاسِ لَا يُؤْمِنُوْنَ ﴿١٧﴾

Aya 15. *Na kama wasiwaitikieni.* Aya hii inaonyesha ya kuwa mashindano waliyotangaziwa wasioamini katika Aya 14 yataendelea hata baada ya Mtume *s.a.w.* Ingekuwa mashindano hayo ni ya siku zile zile za Mtume tu, Allah angesema, "Na kama wasikuitikie." Hivyo Waaislamu wanaambiwa kuwa katika kila zama mnaweza kuwapa makafiri mashindano haya, na mtaona wanashindwa; na Qur'an siku zote itazidi Vitabu vyote katika ubora wake wa namna nyingi; na mtajua ya kuwa bila shaka kimetoka kwa Mungu, maana kama ni kazi ya mwanadamu, basi wanadamu wengine wasingeshindwa kutoa kitu cha namna hii.

Aya 16. *Hawatapunjwa.* Ni wazi katika Aya hii ya kuwa mtu anayefanya bidii kufanikiwa na maisha ya dunia anapata malipo ya juhudi yake na anafanikiwa. Kufanikiwa kwa Wakristo katika dunia hupata kukatolewa ati ndio ushahidi wa ukweli wa dini yao. Aya hii inadhihirisha uwongo wa hoja hii. Mungu anasema, ye yote anayefuata kanuni za dunia hii hawezi kupunguziwa haki yake hata kama yeye haamini.

Aya 18. *Mtu aliye na dalili wazi*, yaani Mtume s.a.w. ambaye ukweli wake na ukweli wa

19. Na ni nani mdhalimu mkubwa kuliko yule amtungiaye Allah uwongo? Hao watahudhurishwa mbele ya Mola wao, na mashahidi watasema: Hawa ndio waliomtungia Mola wao uwongo. Sikilizeni! laana ya Allah iko juu ya wadhalimu;

وَمَنْ اَظْلَمُ مِمَّنِ افْتَرٰى عَلَى اللّٰهِ كَذِبًا ؕ
اُولٰٓئِكَ يُعْرَضُوْنَ عَلٰى رَبِّهِمْ وَيَقُوْلُ
الْاَشْهَادُ هٰٓؤُلَآءِ الَّذِيْنَ كَذَبُوْا عَلٰى
رَبِّهِمْ ۚ اَلَا لَعْنَةُ اللّٰهِ عَلَى الظّٰلِمِيْنَ ۙ﴿۱۹﴾

---

mafundisho aliyoleta umethibitika. *Shahidi mmoja atokaye Kwake atamfuata.* Shahidi hutakiwa kwa ajili ya kuhakikisha jambo. Wakati mafundisho ya Kiislamu yamefanyiwa shaka hasa ni baada ya miaka 1350. Kuna baadhi ya Waislamu wenyewe wanaofikiri mafundisho ya Qur'an, hasa ya Sala tano za kila siku, kukata mikono ya wezi, kuoa wake zaidi ya mmoja, wanawake kufunika nyuso mabarabarani na kutochanganyika ovyo na wanaume wasiokuwa jamaa zao, riba n.k.w. kwamba yanahitaji kubadilishwa. Kuna watu wanaofikiri kuwa Sheria ya Kiislamu imetanguka na wanataka kuleta sheria mpya mahala pake. Kuna hao wapinzani wa Ulaya na Amerika wanaodadisi usahihi wa baadhi ya mambo ya historia yaliyotajwa na Qur'an, na pia wakilaumu kuwa mafunzo mengine ya Qur'an si mazuri kufuata. Mambo kama haya hayakupata kutokea kabla ya zama hizi, na bila shaka kabla yake hapakuwa na haja ya shahidi.

Shahidi huyo aliyefika ni Mjumbe wa Allah, Seyidna Ahmad, Masihi na Mahdi aliyeahidiwa, ambaye alianzisha huu mwendeleo wa Uislamu uitwao Ahmadiyya, wakati ambao mafundisho ya Kiislamu yalipokataliwa na watu waziwazi.

Na kabla yake kulikuwa Kitabu cha Musa ambacho kina bishara nyingi za kufika Mtume *s.a.w.* (tazama maelezo ya sura 7:158). Hizi ndizo dalili tatu za kuhakikisha ukweli wa Mtume *s.a.w.* na ukweli wa dini ya Kiislamu.

Kiongozi na rehema (1) kwa sababu kimewaongoza watu kwenye ukweli wa dini ya Kiislamu, na kimewafanyia rahisi kukubali ukweli wa dini ya Kiislamu kwa kueleza bishara zinazoonyesha ukweli wa Mtume Muhammad *s.a.w.;* (2) kwa sababu kimeweka mizani ya kuhakikisha ukweli wa nabii ye yote; (3) kwa kuwezesha watu kulinganisha mafundisho ya Vitabu viwili; na (4) kwa kusaidia kufafanua kanuni za Sheria.

Ni muhimu kuainisha kijina 'hao' kinamrejea nani. Watu wawili pekee waliotajwa katika aya hii ni Mtukufu Mtume s.a.w. na shahidi kutoka kwa Allah ambaye atamfuata. Ama kumhusu Musa, si yeye bali ni Kitabu chake ndicho chenye kurejewa, na vitabu haviamini. Tunabakiwa na chaguo moja tu kwamba kundi la watu ndilo linalorejewa katika aya hii. Kijina hiki chamrejea siye tu Mtume mwenyewe bali pia mtu aliye chini yake ambaye ni shahidi na baadhi ya watu wengine.

Aya hiyo hapo juu ni lazima ieleweke katika maana hiyo hiyo kwamba siye Mtume tu na shahidi wake ndio wanaouamini ukweli wa Mtume na kuutolea ushuhuda bali idadi kubwa ya wafuasi wao nao pia wanafanya vivyo hivyo.

Ni lazima ikumbukwe kwamba mara nyingine Mitume wakubwa wanatajwa kwa jina la umoja kama mtu mmoja lakini wana uwezekano wa kuzaliana na kusambaa. Hao wanaelezewa kuwa ni 'umma, yaani kundi kubwa la watu ndani ya nafsi zao. Kwa marejeo tazama sura ya 16 aya ya 121.

Baadhi ya watu wamekielewa kijina 'hao' (*uulaaika*) kuwa ni chenye kumrejea Musa na watu wake.

Aya 19. Aya hii inatuambia ya kuwa ni rahisi kabisa kupambanua baina ya mtume mwongo na Mtume mkweli. Mitume wa uwongo ni watu wadhalimu na wako katika laana ya Mungu. Hivyo si vigumu kuwapambanua. Mtu anaweza kuwajua mitume wa uwongo kwa kuona

20. Ambao wanazuilia (watu) njia ya Allah na wanataka ipotoke; na hao ndio wanaoikataa Akhera.

الَّذِيْنَ يَصُدُّوْنَ عَنْ سَبِيْلِ اللّٰهِ وَيَبْغُوْنَهَا عِوَجًا ؕ وَهُمْ بِالْاٰخِرَةِ هُمْ كٰفِرُوْنَ ﴿۱۹﴾

21. Hao hawawezi kamwe kuwaajizisha (watu wa Mungu) ardhini, wala hawana marafiki badala ya Allah; watazidishiwa adhabu mara mbili; hawawezi kusikia wala hawawezi kuona.

اُولٰٓئِكَ لَمْ يَكُوْنُوْا مُعْجِزِيْنَ فِى الْاَرْضِ وَمَا كَانَ لَهُمْ مِّنْ دُوْنِ اللّٰهِ مِنْ اَوْلِيَآءَ ۘ يُضٰعَفُ لَهُمُ الْعَذَابُ ؕ مَا كَانُوْا يَسْتَطِيْعُوْنَ السَّمْعَ وَمَا كَانُوْا يُبْصِرُوْنَ ﴿۲۰﴾

22. Hao ndio wamezihasiri nafsi zao, na yamewapotea waliyokuwa wakiyatunga.

اُولٰٓئِكَ الَّذِيْنَ خَسِرُوْٓا اَنْفُسَهُمْ وَضَلَّ عَنْهُمْ مَّا كَانُوْا يَفْتَرُوْنَ ﴿۲۱﴾

23. Bila shaka hao ndio wenye hasara zaidi katika Akhera.

لَا جَرَمَ اَنَّهُمْ فِى الْاٰخِرَةِ هُمُ الْاَخْسَرُوْنَ ﴿۲۲﴾

24. Hakika wale walioamini na kufanya vitendo vizuri na kunyenyekea kwa Mola wao; hao ndio watu wa Peponi, humo watakaa.

اِنَّ الَّذِيْنَ اٰمَنُوْا وَعَمِلُوا الصّٰلِحٰتِ وَاَخْبَتُوْٓا اِلٰى رَبِّهِمْ ۙ اُولٰٓئِكَ اَصْحٰبُ الْجَنَّةِ ۚ هُمْ فِيْهَا خٰلِدُوْنَ ﴿۲۳﴾

25. Hali ya makundi mawili (haya) ni kama kipofu na kiziwi na aonaye na asikiaye. Je, hawa wawili wanaweza kuwa sawa katika kufanana? Basi je, hamtashika nasaha?

مَثَلُ الْفَرِيْقَيْنِ كَالْاَعْمٰى وَالْاَصَمِّ وَالْبَصِيْرِ وَالسَّمِيْعِ ؕ هَلْ يَسْتَوِيٰنِ مَثَلًا ؕ اَفَلَا تَذَكَّرُوْنَ ﴿۲۴﴾

Neno *Mashahidi* hapa linahusu Mitume ambao watawasuta makafiri kwa kuonyesha hali ya kulaaniwa na mitume wa uwongo, na kuwataka wawalinganishe na kuona tofauti iliyoko.

Aya 20. *Wanataka ipotoke,* yaani iharibike na uzuri wake ufichike kabisa. Maadui wa dini kila mara wanafanya juhudi kubwa ili watu wasipate kujua ubora wa dini ya Mungu. Pia maana yake ni ya kuwa wanataka kuwapoteza watu wanaoshika njia ya haki na kuwaudhi.

Aya 23. *Wenye hasara zaidi,* yaani hao makafiri wanaojaribu kuwatia Manabii wa haki katika hasara duniani, wakumbuke ya kuwa katika Akhera wao hawatakuwa na uwezo hata kidogo wa kuwataabisha Manabii na watu wa haki, bali wao wenyewe ndio watakuwa wenye hasara ya kila namna.

Aya 24. Aya hii inaonyesha ya kuwa imani na vitendo vizuri havitamfaa mtu kwa kupata daraja kubwa za kiroho na ukamilifu mpaka awe na yakini kubwa juu ya Allah na awe na mapenzi naye. Ngazi ya kumfikisha mtu karibu sana na Allah na kumpa utulivu ni upendo na huba kwa Allah, pamoja na imani na vitendo vilivyo sawa na sheria.

FUNGU 2

وَلَقَدْ اَرْسَلْنَا نُوْحًا اِلٰى قَوْمِهٖۤ ۫ اِنِّیْ لَكُمْ
نَذِیْرٌ مُّبِیْنٌ ﴿۲۶﴾

26. Na bila shaka Sisi Tulimtuma Nuhu kwa watu wake, (akawaambia): Hakika mimi kwenu ni Mwonyaji dhahiri.

اَنْ لَّا تَعْبُدُوْۤا اِلَّا اللّٰهَ ؕ اِنِّیْۤ اَخَافُ
عَلَیْكُمْ عَذَابَ یَوْمٍ اَلِیْمٍ ﴿۲۶﴾

27. Ya kwamba msimwabudu ye yote isipokuwa Allah tu; hakika mimi nawahofieni adhabu ya siku iumizayo.

فَقَالَ الْمَلَاُ الَّذِیْنَ كَفَرُوْا مِنْ قَوْمِهٖ مَا
نَرٰىكَ اِلَّا بَشَرًا مِّثْلَنَا وَمَا نَرٰىكَ
اتَّبَعَكَ اِلَّا الَّذِیْنَ هُمْ اَرَاذِلُنَا بَادِیَ
الرَّاْیِ ۚ وَمَا نَرٰى لَكُمْ عَلَیْنَا مِنْ فَضْلٍ
بَلْ نَظُنُّكُمْ كٰذِبِیْنَ ﴿۲۷﴾

28. Hapo wakasema wakubwa wa wale waliokufuru katika kaumu yake: Hatukuoni ila ni mtu tu sawa nasi, wala hatukuoni ila wamekufuata wale waonekanao dhahiri kuwa dhaifu wetu, wala hatuwaoneni kuwa ninyi mnayo fadhili juu yetu, bali tunawaoneni kuwa mu waongo tu.

قَالَ یٰقَوْمِ اَرَءَیْتُمْ اِنْ كُنْتُ عَلٰى بَیِّنَةٍ
مِّنْ رَّبِّیْ وَاٰتٰىنِیْ رَحْمَةً مِّنْ عِنْدِهٖ
فَعُمِّیَتْ عَلَیْكُمْ ؕ اَنُلْزِمُكُمُوْهَا
وَاَنْتُمْ لَهَا كٰرِهُوْنَ ﴿۲۸﴾

29. Akasema: Enyi watu wangu, mwaonaje kama ninayo dalili wazi kutoka kwa Mola wangu, na amenipa rehema kutoka Kwake nayo ikafichikana kwenu; je tutawalazimisheni kuikubali ijapokuwa mwaichukia?

Aya 26. *Mwonyaji abainishaye.* Nabii Nuhu anasema ya kuwa maonyo yangu ni ya dalili. Sikuja kuwaharibu watu au kuwapa tamaa ya bure, bali nimekuja kuwaamsha na kuwadhihirishia haki.

Alama kubwa katika alama za Nabii wa haki ni kuwa yeye anakuwa "Mwonyaji abainishaye," yaani (1) mafundisho yake yanakuwa wazi kabisa, hafanyi kazi kisirisiri wala hafichi mafundisho yake na ujumbe wake kwa watu. Lakini nabii mwongo kila mara anafanya kazi kwa siri, wala hadhihirishi mafundisho yake isije watu wakakosa kuelekea. Siku hizi tazameni jinsi vitabu vya Bab na Bahaullah wa dini ya Bahai vinavyofichwa. Hata vitabu vingine vya Bab vinaharibiwa kabisa na Mababi ili watu wasijue mafundisho yake ya kuipinga dini ya Mungu yalikuwa namna gani.

(2) Nabii wa haki anakuwa na maonyo yabainishayo, yaani yenye dalili, na hivyo maonyo yake hayawapi watu tamaa ya bure. Lakini manabii wa uwongo wanakuwa na maonyo yasiyo na dalili na mwishowe watu wanakata tamaa kabisa.

Aya 28. Aya hii inaonyesha namna wasioamini wanavyopima kuwa Nabii ni mwongo kwa sababu gani. Sababu zao ati ni kwa kuwa Nabii yule ni mtu kama wao, na ya kuwa watu wanaomfuata si watu wa maana. Hivi ndivyo wanavyojidanganya makafiri. Ni wazi kabisa kama wangepima madai ya Mjumbe kwa mizani iliyowekwa na Allah wasingejipoteza namna hii.

وَيٰقَوْمِ لَآ اَسْـَٔلُكُمْ عَلَيْهِ مَالًا ؕ اِنْ
اَجْرِيَ اِلَّا عَلَى اللّٰهِ وَمَآ اَنَا بِطَارِدِ
الَّذِيْنَ اٰمَنُوْا ؕ اِنَّهُمْ مُّلٰقُوْا رَبِّهِمْ
وَلٰكِنِّيْٓ اَرٰىكُمْ قَوْمًا تَجْهَلُوْنَ ﴿٣٠﴾

30. Na enyi watu wangu, siwaombeni mali juu ya (jambo) hili; ujira wangu uko tu kwa Allah; na mimi si mwenye kuwafukuza walioamini; maana wao ndio watakaokutana na Mola wao. Lakini mimi nawaoneni ninyi ni watu mfanyao ujinga.

وَيٰقَوْمِ مَنْ يَّنْصُرُنِيْ مِنَ اللّٰهِ اِنْ
طَرَدْتُّهُمْ ؕ اَفَلَا تَذَكَّرُوْنَ ﴿٣١﴾

31. Na enyi watu wangu, ni nani atakayenisaidia mbele ya Allah ikiwa nitawafukuza? Je, hamfikiri?

وَلَآ اَقُوْلُ لَكُمْ عِنْدِيْ خَزَآئِنُ اللّٰهِ وَلَآ
اَعْلَمُ الْغَيْبَ وَلَآ اَقُوْلُ اِنِّيْ مَلَكٌ وَّلَآ
اَقُوْلُ لِلَّذِيْنَ تَزْدَرِيْٓ اَعْيُنُكُمْ لَنْ
يُّؤْتِيَهُمُ اللّٰهُ خَيْرًا ؕ اَللّٰهُ اَعْلَمُ بِمَا فِيْٓ
اَنْفُسِهِمْ ۖ اِنِّيْٓ اِذًا لَّمِنَ الظّٰلِمِيْنَ ﴿٣٢﴾

32. Wala siwaambieni kuwa ninazo, hazina za Allah; wala sijui mambo ya ghaibu, wala sisemi mimi ni Malaika; wala sisemi kwa wale ambao yanawadharau macho yenu, Allah Hatawapa heri asilan. Allah Anajua sana yaliyomo katika nafsi zao.(Nikisema hivyo) hapo bila shaka nitakuwa miongoni mwa wadhalimu.

قَالُوْا يٰنُوْحُ قَدْ جٰدَلْتَنَا فَاَكْثَرْتَ جِدَالَنَا
فَاْتِنَا بِمَا تَعِدُنَآ اِنْ كُنْتَ مِنَ الصّٰدِقِيْنَ ﴿٣٣﴾

33. Wakasema: Ewe Nuhu, hakika umejadiliana nasi na umezidi mno kujadiliana nasi, basi tuletee unayotuahidi ikiwa u miongoni mwa wakweli.

قَالَ اِنَّمَا يَاْتِيْكُمْ بِهِ اللّٰهُ اِنْ شَآءَ
وَمَآ اَنْتُمْ بِمُعْجِزِيْنَ ﴿٣٤﴾

34. Akasema hakika Allah ataileta kwenu Akipenda, na ninyi hamuwezi kumdhoofisha.

Aya 30. Watakaokutana na Mola wao. Ndiyo kusema nawezaje kuwafukuza hali wao ndio walioamini na hivyo watakuwa na heshima ya kuonana na kukutana na Allah kwa sababu ya utawa na mambo mema wanayoyafanya. Kama ninyi hamwoni heshima yao, basi hili si kosa lao. Aya hii imedhihirisha ya kuwa heshima hasa haiwi kwa mali wala kabila, bali kwa sababu ya imani na kumcha Mungu. Allah amesema, Hakika aheshimiwaye zaidi miongoni mwenu mbele ya Allah ni yule amchaye zaidi katika ninyi (sura 49:14). Pia Mtume s.a.w . akasema "Mungu hatazami sura zenu na mali zenu, bali anatazama mioyo yenu."

Aya 31. Nabii Nuhu anawajibu wasioamini ya kwamba hawezi kuwafukuza waaminio kwa kutaka kuwaridhi wao, licha ya unyonge wao. Hawezi kumchukiza Allah ili kuwapendeza wao.

Aya 34. Aya hii inaeleza kanuni tatu zinazohusu bishara za kuleta adhabu kwa maadui wa Mitume wa Mungu; (1) Wakati wa kufika adhabu huwa kwa desturi hautajwi, Na Mungu tu

35. Wala haitawafalieni nasaha yangu ijapokuwa nataka kuwasihini, kama Allah Anataka kuwaangamizeni. Yeye ndiye Mola wenu; Na Kwake mtarejeshwa.

وَلَا يَنْفَعُكُمْ نُصْحِيْٓ اِنْ اَرَدْتُّ
اَنْ اَنْصَحَ لَكُمْ اِنْ كَانَ اللّٰهُ يُرِيْدُ
اَنْ يُّغْوِيَكُمْ ؕ هُوَ رَبُّكُمْ ۫ وَ اِلَيْهِ
تُرْجَعُوْنَ ﴿۳۵﴾

36. Je, wanasema ameitunga? Sema: Kama nimeitunga, basi kosa langu ni juu yangu, na mimi ni mbali na makosa mnayoyafanya.

اَمْ يَقُوْلُوْنَ افْتَرٰىهُ ؕ قُلْ اِنِ افْتَرَيْتُهٗ
فَعَلَيَّ اِجْرَامِيْ وَاَنَا بَرِيْٓءٌ مِّمَّا
تُجْرِمُوْنَ ﴿۳۶﴾ ع ۴

FUNGU 4

37. Na akafunuliwa Nuhu kwamba hataamini ye yote katika watu wako isipokuwa yule aliyekwisha amini, kwa hiyo usisikitike kwa yale waliyokuwa wakiyatenda.

وَاُوْحِيَ اِلٰى نُوْحٍ اَنَّهٗ لَنْ يُّؤْمِنَ مِنْ
قَوْمِكَ اِلَّا مَنْ قَدْ اٰمَنَ فَلَا تَبْتَىِٕسْ
بِمَا كَانُوْا يَفْعَلُوْنَ ﴿۳۷﴾

---

ndiye Anayeujua; (2) bishara hizo huwa kwa sharti zake na zinaweza kuahirishwa au kubatilishwa namna Mungu atakavyo; (3) mabadiliko yo yote yatakayotokea katika bishara za adhabu, kusudi la Allah halibadiliki, maana wasioamini hawawezi kuzuia kusudi la Allah kutokea.

Aya 36. *Sema: Kama nimeitunga, basi kosa langu ni juu yangu,* Maneno haya yanamhusu Nabii Nuhu na si Mtume *s.a.w.,* Na mradi wake ni kuwa Allah anamwamrisha Nabii Nuhu kuwaambia watu wake ikiwa habari aliyowaambia ni uzushi aliomzulia Mungu, basi bila shaka ataadhibiwa kwa ajili ya uzushi huo, nao hawana haja ya kupata wasiwasi kwa jambo hilo. Lakini kama aliyowaambia ni haki naye ni Mtume wa kweli wa Allah, basi watakuwa wamefanya dhambi kubwa kumkataa, na lazima watahukumiwa kwa kosa hilo.

Aya 37. Aya hii inatuonyesha sababu iliyomfanya awaombee watu wake maangamizo kama inavyooneka katika sura 71:27-28. Katika Aya hii Nuhu anaambiwa ya kwamba hakuna watu wengine watakaoamini katika kaumu yake na hivyo asihuzunikie jambo hilo. Hii inaonyesha ya kwamba mpaka wakati huu alikuwa hajakata tamaa ya watu wake kumkubali, na kila mara aliona wasiwasi juu ya kufuru yao. Hivyo dua aliyoomba inayoonekana katika sura 71:27-28 lazima iwe aliiomba baada ya kupokea habari hii kutoka kwa Allah. Hivyo dua ile ya Nabii Nuhu haikuwa bali kuitikia hukumu iliyokwisha katwa na Allah. Maana, maadamu Mungu Mwenyewe amekwisha kata shauri kuwaangamiza watu wabaya, kuna maana gani Nabii Nuhu naye kuomba waangamizwe? Hivyo dua ya Nuhu ilikuwa na maana ya kwamba Allah apitishe hukumu yake juu ya watu hao.

Mara nyingi inatokea ya kwamba Nabii wa Mungu hata baada ya kujua kuwa Mungu atawaadhibu makafiri anaendelea kuwaombea salama akitumaini ya kwamba Allah anaweza kugeuza shauri lake, na watu wake wanaweza kuamini na kuokoka. Nuhu pia aliendelea kuwaombea heri mpaka alipoona ya kwamba kukawia kwa adhabu yao hakutaleta faida katika dini yake. Basi hapo akaomba Allah apitishe shauri Lake juu ya watu wale.

وَاصْنَعِ الْفُلْكَ بِاَعْيُنِنَا وَوَحْيِنَا وَلَا تُخَاطِبْنِيْ فِي الَّذِيْنَ ظَلَمُوْا ۚ اِنَّهُمْ مُّغْرَقُوْنَ ﴿٣٨﴾

38. Na ukaunde jahazi mbele ya macho Yetu na (iliyo sawa na) ufunuo Wetu. Wala usinizungumze juu ya wale waliodhulumu, kwa yakini wao watazamishwa.

وَيَصْنَعُ الْفُلْكَ ۖ وَكُلَّمَا مَرَّ عَلَيْهِ مَلَاٌ مِّنْ قَوْمِهٖ سَخِرُوْا مِنْهُ ۭ قَالَ اِنْ تَسْخَرُوْا مِنَّا فَاِنَّا نَسْخَرُ مِنْكُمْ كَمَا تَسْخَرُوْنَ ﴿٣٩﴾

39. Na yeye alikuwa anaunda jahazi; na kila walipompita wakuu wa watu wake walimcheka; akasema: Kama ninyi mnatucheka, hakika nasi (pia) tutawachekeni kama mnavyotucheka.

فَسَوْفَ تَعْلَمُوْنَ ۙ مَنْ يَّاْتِيْهِ عَذَابٌ يُّخْزِيْهِ وَيَحِلُّ عَلَيْهِ عَذَابٌ مُّقِيْمٌ ﴿٤٠﴾

40. Basi karibuni mtajua ni nani itakayemfikia adhabu ya kumfedhehesha na itamteremkia adhabu ikaayo.

حَتّٰٓى اِذَا جَاۗءَ اَمْرُنَا وَفَارَ التَّنُّوْرُ ۙ قُلْنَا احْمِلْ فِيْهَا مِنْ كُلٍّ زَوْجَيْنِ اثْنَيْنِ وَاَهْلَكَ اِلَّا مَنْ سَبَقَ عَلَيْهِ الْقَوْلُ وَمَنْ اٰمَنَ ۭ وَمَآ اٰمَنَ مَعَهٗٓ اِلَّا قَلِيْلٌ ﴿٤١﴾

41. Hata ilipofika amri Yetu na chemchem zikababujika, Tukamwambia: Pakia humo katika kila wanyama jozi moja jike na dume, na na ahali zako - isipokuwa yule ambaye ime-mpitia hukumu - na walioamini. Na hawakuamini pamoja naye ila wachache tu.

Na hata kama ikubaliwe ya kwamba Nabii Nuhu alimwomba Mungu watu wake waangamizwe, hatapata ila yo yote, maana dua inayoombwa kwa amri ya Allah haiwezi kupunguza heshima ya Mtume wa Mungu.

Aya 38. *Mbele ya macho Yetu.* Maneno haya yalivyo kwa kiarabu yana maana nyingi kwa kufuata maana ya neno 'ain, na katika hizo moja ni, "Katika ulinzi wetu" (Mufradat). Kwa hakika majahazi mawili - moja la dhahiri na jingine la undani - yaliundwa na Nabii Nuhu. Jahazi la dhahiri ndilo lile la mbao na Misumari, na la undani ni mafundisho yake ambayo kwa kuokoka ilikuwa ni lazima mtu ayafuate, na wale tu walioyafuata ndio waliosalimika.

Wala usinizungumze juu ya wale waliodhulumu. Maneno haya pia yanaonyesha ya kuwa dua ya maangamizo ya Nabii Nuhu iliyomo katika sura 71:27-28 hakuiomba kwa kutaka kwake mwenyewe, maana kama yeye mwenyewe ndiye aliwaombea watu waovu kuangamizwa, hapakuwa sababu Mwenyezi Mungu kumkataza kuwaombea waachwe.

Aya 41. Ikumbukwe ya kuwa adhabu iliyowafikia watu wa Nabii Nuhu ilikuwa ya maji kutoka juu na chini. Sura 54:12, 13 inatufahamisha ya kuwa mvua pia zilinyesha na chemchem zikatoa maji.

Katika kila wanyama. Neno la Kiarabu kullin mradi wake ni kila namna ya wanyama aliowahitaji, siyo wanyama wote wa mjini na porini. Kadhalika safina ile haikuwa kubwa ya kutosha kuchukua jozi ya kila namna ya wanyama.

42. Na akasema: Pandeni humo, kwa jina la Allah kuwe kwenda kwake na kusimama kwake. Hakika Mola wangu ni Msamehevu sana Mrehemevu.

وَقَالَ ارْكَبُوْا فِيْهَا بِسْمِ اللّٰهِ مَجْرٖىهَا
وَمُرْسٰىهَا ؕ اِنَّ رَبِّيْ لَغَفُوْرٌ رَّحِيْمٌ ﴿٤١﴾

43. Nayo ilikwenda nao katika mawimbi kama milima. Na Nuhu akamwita mwanawe aliyekuwa upande mwingine: Ewe mwanangu panda pamoja nasi wala usiwe pamoja na makafiri.

وَهِيَ تَجْرِيْ بِهِمْ فِيْ مَوْجٍ كَالْجِبَالِ
وَنَادٰى نُوْحُ ابْنَهٗ وَكَانَ فِيْ مَعْزِلٍ يّٰبُنَيَّ
ارْكَبْ مَّعَنَا وَلَا تَكُنْ مَّعَ الْكٰفِرِيْنَ ﴿٤٢﴾

44. Akasema: Sasa hivi nitaukimbilia mlima utakaonilinda na maji. Akasema: Hakuna leo wa kulinda na amri ya Allah isipokuwa yule Atakayemrehemu. Mara wimbi likaingia kati yao na akawa miongoni mwa waliogharikishwa.

قَالَ سَاٰوِيْٓ اِلٰى جَبَلٍ يَّعْصِمُنِيْ مِنَ
الْمَآءِ ؕ قَالَ لَا عَاصِمَ الْيَوْمَ مِنْ اَمْرِ اللّٰهِ
اِلَّا مَنْ رَّحِمَ ۚ وَحَالَ بَيْنَهُمَا الْمَوْجُ
فَكَانَ مِنَ الْمُغْرَقِيْنَ ﴿٤٣﴾

45. Na ikasemwa: Ewe ardhi! meza maji yako, na Ewe mbingu jizuie, na maji yakazama, na amri ikatolewa, na (jahazi) likasimama juu ya Judi. na ikasemwa: Ni maangamizo kwa watu wadhalimu.

وَقِيْلَ يٰٓاَرْضُ ابْلَعِيْ مَآءَكِ وَيٰسَمَآءُ
اَقْلِعِيْ وَغِيْضَ الْمَآءُ وَقُضِيَ الْاَمْرُ
وَاسْتَوَتْ عَلَى الْجُوْدِيِّ وَقِيْلَ بُعْدًا
لِّلْقَوْمِ الظّٰلِمِيْنَ ﴿٤٤﴾

Aya 42. *Kwa jina la Allah kuwe kwenda kwake na kusimama kwake.* Waislamu wamekuwa na desturi ya kuomba maombi haya yanayotajwa katika Aya hii wanapopanda majahazi, meli n.k.w.

Aya 43. *Ewe mwanangu.* Wafasiri wamehitilafiana juu ya mwana aliyetajwa hapa kama alikuwa mwana hasa wa Nabii Nuhu au jamaa tu. Lakini wengi walio mashuhuri kama Ibni Mas'ud, Ibni Abbas, Ikrima na Adh-Dhahhaak, Ibni Jubair na wengineo wanakubali wa kuwa mwana huyo alikuwa mwana hasa wa Nabii Nuhu.

Aya 44. *Nitaukimbilia mlima.* Maneno haya yanaonyesha mahali pa Nabii Nuhu palikuwa na milima.

Utakaonilinda na maji, ni maneno yanayoonyesha namna watu washupavu wanavyofumba macho yao juu ya mambo yaliyo dhahiri kabisa. Maji yanazidi kukua, lakini mwanawe Nuhu bado anafanyia shaka ukweli wa Ujumbe wa baba yake.

Aya 45. *(Jahazi) likasimama juu ya Judi.* Yakut Al-Hamwi anaeleza ya kuwa mlima Judi ni mfuatano mrefu wa milima upande wa mashariki wa Tigris katika jimbo la Mosul (Mu'jam).

وَنَادٰى نُوْحٌ رَّبَّهٗ فَقَالَ رَبِّ اِنَّ ابْنِيْ
مِنْ اَهْلِيْ وَاِنَّ وَعْدَكَ الْحَقُّ وَاَنْتَ
اَحْكَمُ الْحٰكِمِيْنَ ﴿٤٦﴾

46. Na (hapo) Nuhu akamwita Mola wake na akasema: Ee Mola wangu! hakika mwanangu ni katika ahali zangu, na hakika ahadi Yako ni haki; nawe ni Hakimu bora kuliko mahakimu wote.

قَالَ يٰنُوْحُ اِنَّهٗ لَيْسَ مِنْ اَهْلِكَ ۚ اِنَّهٗ
عَمَلٌ غَيْرُ صَالِحٍ ۖ فَلَا تَسْـَٔلْنِ مَا لَيْسَ
لَكَ بِهٖ عِلْمٌ ؕ اِنِّيْۤ اَعِظُكَ اَنْ تَكُوْنَ
مِنَ الْجٰهِلِيْنَ ﴿٤٧﴾

47. Akasema: Ewe Nuhu, hakika huyo si miongoni mwa ahali zako; hakika yeye ni (mwenye) mwendo usio mzuri. Basi usiniombe usiyoyajua. Mimi nakunasihi usije ukawa miongoni mwa wajinga.

قَالَ رَبِّ اِنِّيْۤ اَعُوْذُ بِكَ اَنْ اَسْـَٔلَكَ مَا
لَيْسَ لِيْ بِهٖ عِلْمٌ ؕ وَاِلَّا تَغْفِرْ لِيْ
وَتَرْحَمْنِيْۤ اَكُنْ مِّنَ الْخٰسِرِيْنَ ﴿٤٨﴾

48. (Nuhu) akasema: Ee Mola wangu, hakika mimi najikinga Kwako nisije kukuomba nisiyoyajua; na kama Hutanisamehe na kunirehemu, nitakuwa miongoni mwa wapatao hasara.

قِيْلَ يٰنُوْحُ اهْبِطْ بِسَلٰمٍ مِّنَّا وَبَرَكٰتٍ
عَلَيْكَ وَعَلٰۤى اُمَمٍ مِّمَّنْ مَّعَكَ ؕ وَاُمَمٌ
سَنُمَتِّعُهُمْ ثُمَّ يَمَسُّهُمْ مِّنَّا عَذَابٌ
اَلِيْمٌ ﴿٤٩﴾

49. Ikasemwa: Ewe Nuhu, shuka kwa salama itokayo Kwetu na kwa baraka zilizo juu yako na juu ya watu walio pamoja nawe. Na wako baadhi ya watu hivi karibuni Tutawafaidisha, kisha itawashika kutoka Kwetu adhabu iumizayo.

Aya 46. Nabii Nuhu kwa kukosa kuzingatia vizuri, alifikiri kwamba watu wote wa nyumbani mwake watapona katika gharika. Lakini alipoona mwanawe anatota, akaomba kwa adabu sana akimkumbusha Mungu ahadi aliyompa, na papo anakiri ya kwamba huenda amekosa kufahamu ahadi ile makusudi yake, kwa vile ahadi za Mungu huwa haki.

Aya 47. *Huyo si miongoni mwa ahali zako.* Yaani, Allah alipoahidi kuwaokoa ahali zake, mradi wake si wote, bali wale wale waliomwamini yeye.

Ni (mwenye) mwenendo usio mzuri. Hii ni namna moja ya kufasiri maneno *innahuu 'amalun ghairu saalihin.* Maneno haya pia yanaweza kufasiriwa, "Hakika maombi hayo ni tendo lisilo zuri," maana wakati wa kuomba umekwisha na hukumu ya kugharikishwa kwake imekwisha katwa.

Aya 48. *Na kama Hutanisamehe.* Ni wazi Nabii Nuhu hakufanya kosa lo lote la kuvunja amri, bali ilikuwa kutofahamu tu, lakini hata hivyo anaomba ghofira. Hii inaonyesha kwamba neno *istighfaar* linapotumika kwa ajili ya Mitume linakuwa halina maana ya kusamehewa dhambi, bali linakuwa na maana ya kulindwa na matokeo mabaya ya unyonge na udhaifu wa kibinadamu.

تِلْكَ مِنْ اَنْۢبَآءِ الْغَيْبِ نُوْحِيْهَآ اِلَيْكَ ۚ مَا كُنْتَ تَعْلَمُهَآ اَنْتَ وَلَا قَوْمُكَ مِنْ قَبْلِ هٰذَا ۛ فَاصْبِرْ ۛ اِنَّ الْعَاقِبَةَ لِلْمُتَّقِيْنَ ﴿٤٩﴾

50. Hizi ni katika habari za siri Tunazokufunulia. Hukuwa unazijua, wewe wala watu wako, kabla ya hii. Basi subiri, hakika mwisho (mwema) ni kwa wamchao Mungu.

FUNGU 5

وَاِلٰى عَادٍ اَخَاهُمْ هُوْدًا ۛ قَالَ يٰقَوْمِ اعْبُدُوا اللّٰهَ مَا لَكُمْ مِّنْ اِلٰهٍ غَيْرُهٗ ۛ اِنْ اَنْتُمْ اِلَّا مُفْتَرُوْنَ ﴿٥٠﴾

51. Na kwa Waadi (Tulimtuma) ndugu yao Hudi. Akasema: Enyi watu wangu! Mwabuduni Allah; ninyi hamna Mungu isipokuwa Yeye. Ninyi ni watungao uwongo tu.

يٰقَوْمِ لَآ اَسْـَٔلُكُمْ عَلَيْهِ اَجْرًا ۛ اِنْ اَجْرِيَ اِلَّا عَلَى الَّذِيْ فَطَرَنِيْ ۛ اَفَلَا تَعْقِلُوْنَ ﴿٥١﴾

52. Enyi watu wangu, siwaombeni ujira juu ya hayo; sina ujira isipokuwa kwa Yule Aliyeniumba: basi je, hamfahamu?

وَيٰقَوْمِ اسْتَغْفِرُوْا رَبَّكُمْ ثُمَّ تُوْبُوْٓا اِلَيْهِ يُرْسِلِ السَّمَآءَ عَلَيْكُمْ مِّدْرَارًا وَّيَزِدْكُمْ قُوَّةً اِلٰى قُوَّتِكُمْ وَلَا تَتَوَلَّوْا مُجْرِمِيْنَ ﴿٥٢﴾

53. Na enyi watu wangu! ombeni msamaha kwa Mola wenu, kisha mtubie Kwake, Atawaleteeni mawingu yatiririshayo mvua tele, na Atawazidishieni nguvu zenu. Wala msigeuke kuwa wakosefu.

قَالُوْا يٰهُوْدُ مَا جِئْتَنَا بِبَيِّنَةٍ وَّمَا نَحْنُ بِتَارِكِيْٓ اٰلِهَتِنَا عَنْ قَوْلِكَ وَمَا نَحْنُ لَكَ بِمُؤْمِنِيْنَ ﴿٥٣﴾

54. Wakasema: Ewe Hud! hujatuletea dalili iliyo wazi, wala sisi si wenye kuiacha miungu yetu kwa usemi wako, wala sisi si wenye kukuamini.

اِنْ نَّقُوْلُ اِلَّا اعْتَرٰىكَ بَعْضُ اٰلِهَتِنَا

55. Hatusemi ila baadhi ya miungu yetu imekutia balaa. Akasema: Hakika

Aya 50. *Hizi ni katika habari za siri,* yaani si kama tunakusimulia habari hizi ziwe visa, bali ni bishara zitakazotimia kwako na kwa watu wako, kama zilivyotimizwa kwa watu wa Nabii Nuhu; yaani mwishoni wacha-Mungu walishinda.

Aya 53. Aya hii inaonyesha kuwa kazi kubwa ya Waadi ilikuwa ukulima, wakitegemea mvua tu, bila visima na mifereji ya kumwagia maji mashambani. Aya hii pia inaonyesha ya kuwa watu wakimkubali Nabii, Mungu anawafanyia vizuri hali zao si za kidini tu bali pia za kidunia.

Aya 55. *Namshahidisha Allah.* Yaani, ninyi mmekataa mambo yaliyo sawa na akili. Hivyo sasa namwomba Allah apambanue baina ya ukweli na uwongo kwa Ishara zenye nguvu zitokazo mbinguni.

mimi namshahidisha Allah nanyi shuhudieni ya kwamba mimi niko mbali na hiyo mnayoishirikisha.

56. Kinyume Chake. Basi nyote nifanyieni hila kisha msinipe muhula.

57. Hakika mimi nimemtegemea Allah, Mola wangu na Mola wenu. Hakuna mnyama ye yote isipokuwa Yeye Amelishika panja lake. Bila shaka Mola wangu Yu juu ya njia iliyonyoka.

58. Na kama mtarudi nyuma, basi nimekwisha wafikishieni niliyotumwa nayo kwenu, na Mola wangu Atawafanya makhalifa watu wengine ghairi yenu, wala ninyi hamtaweza kumdhuru hata kidogo. Hakika Mola wangu ni Mhifadhi wa kila kitu.

59. Na ilipofika amri Yetu, Tukamwokoa Hudi na wale walioamini pamoja naye kwa rehema itokayo Kwetu. Na Tukawaokoa katika adhabu ngumu.

بِسُوْٓءٍ ؕ قَالَ اِنِّیْٓ اُشْهِدُ اللّٰهَ وَاشْهَدُوْٓا
اَنِّیْ بَرِیْٓءٌ مِّمَّا تُشْرِكُوْنَ ۙ﴿۵۵﴾
مِنْ دُوْنِهٖ فَكِیْدُوْنِیْ جَمِیْعًا ثُمَّ
لَا تُنْظِرُوْنِ﴿۵۶﴾
اِنِّیْ تَوَكَّلْتُ عَلَی اللّٰهِ رَبِّیْ وَ رَبِّكُمْ ؕ
مَا مِنْ دَآبَّةٍ اِلَّا هُوَ اٰخِذٌۢ بِنَاصِیَتِهَا ؕ
اِنَّ رَبِّیْ عَلٰی صِرَاطٍ مُّسْتَقِیْمٍ﴿۵۷﴾
فَاِنْ تَوَلَّوْا فَقَدْ اَبْلَغْتُكُمْ مَّآ اُرْسِلْتُ بِهٖٓ
اِلَیْكُمْ ؕ وَ یَسْتَخْلِفُ رَبِّیْ قَوْمًا غَیْرَكُمْ ۚ
وَلَا تَضُرُّوْنَهٗ شَیْـًٔا ؕ اِنَّ رَبِّیْ عَلٰی
كُلِّ شَیْءٍ حَفِیْظٌ﴿۵۸﴾
وَلَمَّا جَآءَ اَمْرُنَا نَجَّیْنَا هُوْدًا وَّ الَّذِیْنَ
اٰمَنُوْا مَعَهٗ بِرَحْمَةٍ مِّنَّا ۚ وَ نَجَّیْنٰهُمْ مِّنْ
عَذَابٍ غَلِیْظٍ﴿۵۹﴾

Niko mbali na hiyo mnayoishirikisha. Hili ndilo jibu Nabii Hudi alilowapa watu wake waliposema kuwa miungu yao imemtia balaa na kuiharibu akili yake. Anawaambia ya kwamba, ikiwa wanadhani kuwa ni miungu yao imemharibu akili basi yeye anaikusanya miungu yao yote na kuikadhibisha na kadhalika desturi zao za uovu, na sasa miungu yao na imfanye vibaya iwezavyo.

Aya 57. *Mola wangu na Mola wenu*. Nabii Hudi kwa maneno haya anataka kuwaambia ya kwamba Mola wenu ni Rafiki yangu na Msaidizi wangu, basi nitawezaje kuwaogopa ninyi watumishi wake, kwani watumishi hawana uwezo wa kumdhuru rafiki wa bwana wao.

Amelishika panja lake. Maneno haya yanahusu desturi ya zamani ya Waarabu. Watu waliposhindwa vitani na kuletwa mbele ya walioshinda, basi mshindi alimshika nywele za paji la uso na kumtikisa kuonyesha ushindi wake. Desturi nyingine miongoni mwao ilikuwa ya kwamba mshindi alipotaka kuwahurumia walioshindwa, aliyanyoa mapanja yao na kuwaacha huru. Hivyo, kifungu hicho cha maneno kina maana zote mbili. Maana yake inaweza kuwa ya kwamba kila mwanadamu yuko chini ya mamlaka na ulinzi wa Allah; au ya kwamba Mungu amemfadhili mwanadamu kwa kumwumba huru. Hivyo Qur'an inamkumbusha mwanadamu ya kwamba yuko katika mamlaka ya Mwenyezi Mungu , na ni kwa fadhili na hisani Zake yeye amepewa maisha ya uhuru; ambapo kwa sababu ya dhambi zake anakuwa hana haki ya uhuru huo.

Aya 58. Maadui wa Manabii wa Mungu katika ujinga wao hudhani wakikataa ujumbe wa Mtume watakuwa wamemdhuru. Hapa Nabii Hudi anawaambia, taabu ya kukataa ujumbe anaweza

وَتِلْكَ عَادٌ ۗ جَحَدُوْا بِاٰيٰتِ رَبِّهِمْ وَعَصَوْا رُسُلَهٗ وَاتَّبَعُوْٓا اَمْرَ كُلِّ جَبَّارٍ عَنِيْدٍ ﴿٦٠﴾

60. Na hao ndio Waadi. Walikanusha Aya za Mola wao, na wakawaasi Mitume Wake, na wakafuata amri ya kila jabari, adui ya haki.

وَاُتْبِعُوْا فِيْ هٰذِهِ الدُّنْيَا لَعْنَةً وَّيَوْمَ الْقِيٰمَةِ ۗ اَلَآ اِنَّ عَادًا كَفَرُوْا رَبَّهُمْ ۗ اَلَا بُعْدًا لِّعَادٍ قَوْمِ هُوْدٍ ﴿٦١﴾

61. Na wakafuatishiwa laana katika dunia hii na siku ya Kiyama. Sikilizeni! Hakika Waadi walimkufuru Mola wao. Sikilizeni! Maangamizo kwa Waadi, kaumu ya Hudi.

FUNGU 6

وَاِلٰى ثَمُوْدَ اَخَاهُمْ صٰلِحًا ۘ قَالَ يٰقَوْمِ اعْبُدُوا اللّٰهَ مَا لَكُمْ مِّنْ اِلٰهٍ غَيْرُهٗ ۗ هُوَ اَنْشَاَكُمْ مِّنَ الْاَرْضِ وَاسْتَعْمَرَكُمْ فِيْهَا فَاسْتَغْفِرُوْهُ ثُمَّ تُوْبُوْٓا اِلَيْهِ ۗ اِنَّ رَبِّيْ قَرِيْبٌ مُّجِيْبٌ ﴿٦٢﴾

62. Na kwa Wathamudi (Tukamtuma) ndugu yao Saleh. Akasema: Enyi watu wangu, Mwabuduni Allah; ninyi hamna Mungu ghairi Yake. Yeye ndiye Aliyewakuzeni katika ardhi, na Akawakalisheni humo. Basi Mwombeni msamaha, kisha Mwelekeeni. Hakika Mola wangu Yu karibu, Mwenye kukubali (maombi).

قَالُوْا يٰصٰلِحُ قَدْ كُنْتَ فِيْنَا مَرْجُوًّا قَبْلَ هٰذَآ اَتَنْهٰىنَآ اَنْ نَّعْبُدَ مَا يَعْبُدُ اٰبَآؤُنَا وَاِنَّنَا لَفِيْ شَكٍّ مِّمَّا تَدْعُوْنَآ اِلَيْهِ مُرِيْبٍ ﴿٦٣﴾

63. Wakasema: Ewe Saleh! bila shaka ulikuwa mwenye kutegemewa kati yetu kabla ya haya. Je, unatukataza kuabudu waliowaabudu baba zetu? Na hakika sisi tumo katika shaka ihangaishayo kwa hayo unayotuitia.

---

kuipata anayepelekewa ujumbe huo au aliyeutuma. Mimi ni mchukuzi tu. Mungu aliyeuleta ujumbe hawezi kupata taabu maana Yeye ni Mwenye nguvu kabisa. Wenye taabu ni wale wenye kuukataa, na baada ya hapo ujumbe wa Mungu haufi bure, ila Mungu atawaleta watakao ukubali.

Aya 60. Neno *tilka* (hao) linaonyesha ukuu na utukufu wa kidunia wa kabila la Waadi. Limetumiwa kudokeza ya kwamba ingawa Waadi walikuwa watu wenye nguvu lakini walipofanya kiburi na uovu na kukataa ujumbe wa Allah, waliangamia.

Aya 61. *Laana.* Mungu anapotoa laana maana yake inakuwa "kufukuzilia mbali" au "Kutupa mbali na rehema." Katika maana hii sehemu ya kwanza ya Aya maana yake itakuwa Allah atawaondoa au kuwatupa mbali wasioamini siku ya Kufufuka.

Aya 63. Watu wa Nabii Saleh hapa wanasikitika ya kwamba walikuwa wanatazamia mtu mwenye akili na sifa njema kama Saleh atawaletea mafanikio; lakini anataka kuwaangamiza kwa

64. Akasema: Enyi watu wangu! mwaonaje kama niko kwenye dalili wazi itokayo kwa Mola wangu, naye Amenipa rehema kutoka Kwake, basi ni nani atakayenisaidia kwa Allah kama nikimwasi? Basi hapo hamtanizidishia ila hasara.

قَالَ يٰقَوْمِ اَرَءَيْتُمْ اِنْ كُنْتُ عَلٰى بَيِّنَةٍ
مِّنْ رَّبِّيْ وَاٰتٰنِيْ مِنْهُ رَحْمَةً فَمَنْ يَّنْصُرُنِيْ
مِنَ اللّٰهِ اِنْ عَصَيْتُهٗ ۫ فَمَا تَزِيْدُوْنَنِيْ
غَيْرَ تَخْسِيْرٍ ﴿٦٣﴾

65. Na enyi watu wangu, huyu ngamia wa Allah ni Ishara kwenu, basi mwacheni ale katika ardhi ya Allah, wala msimguse kwa ubaya isije ikawashikeni adhabu iliyo karibu.

وَيٰقَوْمِ هٰذِهٖ نَاقَةُ اللّٰهِ لَكُمْ اٰيَةً فَذَرُوْهَا
تَاْكُلْ فِيْٓ اَرْضِ اللّٰهِ وَلَا تَمَسُّوْهَا بِسُوْٓءٍ
فَيَاْخُذَكُمْ عَذَابٌ قَرِيْبٌ ﴿٦٤﴾

66. Lakini wao walimkata miguu yake; basi (Saleh) akasema, Jifurahisheni majumbani mwenu kwa siku tatu; hiyo ni ahadi isiyokadhibishwa.

فَعَقَرُوْهَا فَقَالَ تَمَتَّعُوْا فِيْ دَارِكُمْ
ثَلٰثَةَ اَيَّامٍ ۭ ذٰلِكَ وَعْدٌ غَيْرُ مَكْذُوْبٍ ﴿٦٥﴾

---

kuwakataza kuabudu vilivyokuwa vinaabudiwa na wazee wao. Jambo hili likawatia wasiwasi sana.

Maneno hayo ya juu waliyomwambia Saleh si ya kumsifu uwongo uwongo, bali hasa, kama walivyo Manabii wote, watu wake walimtumainia sana kwa ajili ya vipawa vyake vya ajabu na mwenendo mtukufu wa tabia. Hivi ndivyo alivyokuwa Mtume *s.a.w.,* Abu Bakar, Ali, Zaid na Khadija (Radhi ya Mungu iwe juu yao) walimwamini kabla hawajawa na habari nyingi za mafundisho yake, na kabla hawajaona Ishara yo yote ya kumsadikisha. Walimkubali kwa ushahidi wa maisha yake yaliyokuwa safi.

Aya 65. Hadithi nyingi zimebuniwa na watu juu ya huyu ngamia jike wa Nabii Saleh. Katika Qur'an hakuna cho chote kinachokubalisha hadithi hizo. Kwa mfano, hadithi moja iliyobuniwa ni kwamba ngamia huyo alitoka katika mwamba wa jiwekimwujiza wakati Nabii Saleh alipoambiwa na watu wake afanye mwujiza na Nabii Saleh akaomba kwa Mungu, basi ngamia huyo akatoka ndani ya mwamba. Wanasema mara tu alipotoka katika huo mwamba alipata mimba na akazaa pale pale. Qur'an haielezi mahali po pote kuwa ngamia yule alitokea kimwujiza. Kinyume cha hayo katika sura 26:154 na 159 inaonekana ya kuwa kuzaliwa kwa ngamia jike yule hakukuwa kinyume na desturi, bali Ishara kwao ilikuwa ni kuwa huru ngamia yule. Kama kutokea kwa ngamia yule kungekuwa kwa kimwujiza kama wasemavyo wasimuliaji hadithi, Nabii Saleh alipoambiwa na watu wake aonyeshe Ishara , angewarejesha kwenye habari za ngamia yule jinsi alivyotoka mzima-mzima ndani ya jiwe, akapata mimba na kuzaa wakati ule ule. Lakini anawajibu ya kwamba wataona Ishara kama hawatamwacha ngamia kufanya atakavyo.

Aya 66. Kila namna ya hadhari aliyofanya Nabii Saleh haikufaa kitu. Maadui zake wakampiga ngamia wake na kumwua. Hivyo ikawa wameitukana ilani ya Allah, basi adhabu waliyoonywa nayo ikawashukia.

فَلَمَّا جَآءَ اَمۡرُنَا نَجَّيۡنَا صٰلِحًا وَّالَّذِيۡنَ اٰمَنُوۡا مَعَهٗ بِرَحۡمَةٍ مِّنَّا وَمِنۡ خِزۡيِ يَوۡمِئِذٍ ؕ اِنَّ رَبَّكَ هُوَ الۡقَوِيُّ الۡعَزِيۡزُ ﴿۶۶﴾

67. Basi ilipofika amri Yetu, Tukamwokoa Saleh na wale walioamini pamoja naye kwa rehema Yetu, na pia (Tukawaokoa) katika fedheha ya siku hiyo. Hakika Mola wako ndiye Mwenye nguvu, Ashindaye.

وَاَخَذَ الَّذِيۡنَ ظَلَمُوا الصَّيۡحَةُ فَاَصۡبَحُوۡا فِىۡ دِيَارِهِمۡ جٰثِمِيۡنَ ﴿۶۷﴾ۙ

68. Na adhabu ikawashika wale waliodhulumu na asubuhi kulipopambazuka wakawa wameanguka kifudifudi ndani ya majumba yao.

كَاَنۡ لَّمۡ يَغۡنَوۡا فِيۡهَا ؕ اَلَا اِنَّ ثَمُوۡدَا كَفَرُوۡا رَبَّهُمۡ ؕ اَلَا بُعۡدًا لِّثَمُوۡدَ ﴿۶۸﴾ ع

69. Kana kwamba hawakuwamo. Sikilizeni! hakika Wathamudi walimkufuru Mola wao; fahamuni! ni maangamio kwa Wathamudi!

FUNGU 7

وَلَقَدۡ جَآءَتۡ رُسُلُنَاۤ اِبۡرٰهِيۡمَ بِالۡبُشۡرٰى قَالُوۡا سَلٰمًا ؕ قَالَ سَلٰمٌ فَمَا لَبِثَ اَنۡ جَآءَ بِعِجۡلٍ حَنِيۡذٍ ﴿۶۹﴾

70. Na bila shaka Wajumbe Wetu walimwendea Ibrahimu kwa habari njema (na) wakasema: Salaam. Akasema: (Juu yenu pia iwe) salaam, na hakukaa ila akaleta ndama aliyeokwa.

فَلَمَّا رَاۤ اَيۡدِيَهُمۡ لَا تَصِلُ اِلَيۡهِ نَكِرَهُمۡ وَاَوۡجَسَ مِنۡهُمۡ خِيۡفَةً ؕ قَالُوۡا لَا تَخَفۡ اِنَّاۤ اُرۡسِلۡنَاۤ اِلٰى قَوۡمِ لُوۡطٍ ﴿۷۰﴾ؕ

71. Lakini alipoona mikono yao haikifikii (chakula), akawachukulia kuwa ni wageni, na akawaonea hofu. Wakasema: Usiogope, kwani sisi tumetumwa kwa watu wa Luti.

Aya 70. Nabii Ibrahimu, Baba wa Manabii, alikuwa mtoto wa Terah, Alizaliwa mahali panapoitwa Ur ya Chaldea. Ni vigumu kusema ni lini hasa aliishi. Inasemekana aliishi kwa umri wa miaka 175. Ibrahimu ni babu wa mataifa mawili, Waisraeli na Waismaili, ambao wote wanamheshimu sana. Jina hasa la Nabii Ibrahim lilikuwa Abram, lakini baada ya kumzaa Ismaili akaitwa Ibrahim yaani "Baba wa makundi ya watu" au "Baba wa mataifa mengi." Kundi moja la wazao wake, Waisraeli, waliishi Kanaan, na Waismaili katika Bara Arabu. Ili kutimiza ndoto yake maarufu, Nabii Ibrahimu alimchukua mwanawe Ismaili na mkewe Hajira akawapeleka katika jangwa la Bara Arabu ambako wazao wa Ismaili walikua na kuzaliana na ambako wakati ulipotimia, akazaliwa Mtume Muhammad *s.a.w.* sawa na ahadi ambayo Mungu alimpa Nabii Ibrahimu. Mtume Muhammad *s.a.w.* mwenyewe alisema *Anaa da'watu Ibraahiimu, yaani,* "Mimi ni dua ya Ibrahimu" (Asakir).

Aya 71. *Akawaonea hofu.* Hakuwaonea hofu kwamba aliwaogopa, bali alidhani hakuwafanyia adabu nzuri inayowastahili wageni, basi akahofu isiwe jambo hilo limetokea, ndiyo maana wageni wake hawali.

وَامۡرَاَتُهٗ قَآئِمَةٌ فَضَحِكَتۡ فَبَشَّرۡنٰهَا بِاِسۡحٰقَ ۙ وَمِنۡ وَّرَآءِ اِسۡحٰقَ يَعۡقُوۡبَ ﴿۷۱﴾

72. Na mkewe alikuwa amesimama, naye akacheka, Tukampa habari njema ya (kuzaliwa) Isihaka, na baada ya Isihaka, Yaakubu.

قَالَتۡ يٰوَيۡلَتٰٓى ءَاَلِدُ وَاَنَا عَجُوۡزٌ وَّهٰذَا بَعۡلِىۡ شَيۡخًا ؕ اِنَّ هٰذَا لَشَىۡءٌ عَجِيۡبٌ ﴿۷۲﴾

73. (Mkewe Ibrahimu) akasema: Miye wao! Je, nitazaa na hali mimi ni mkongwe na huyu mume wangu ni mzee sana? Hakika hili ni jambo la ajabu!

قَالُوۡۤا اَتَعۡجَبِيۡنَ مِنۡ اَمۡرِ اللّٰهِ ؕ رَحۡمَتُ اللّٰهِ وَبَرَكٰتُهٗ عَلَيۡكُمۡ اَهۡلَ الۡبَيۡتِ ؕ اِنَّهٗ حَمِيۡدٌ مَّجِيۡدٌ ﴿۷۳﴾

74. Wakasema: Je, unastaajabia amri ya Allah? Rehema ya Allah na baraka zake ziko juu yenu, enyi watu wa nyumba hii! Hakika Yeye ndiye Asifiwaye, Atukuzwaye.

فَلَمَّا ذَهَبَ عَنۡ اِبۡرٰهِيۡمَ الرَّوۡعُ وَجَآءَتۡهُ الۡبُشۡرٰى يُجَادِلُنَا فِىۡ قَوۡمِ لُوۡطٍ ؕ ﴿۷۴﴾

75. Basi hofu ilipomwondoka Ibrahimu, na imemfikia habari njema, akaanza kujadiliana nasi juu ya watu wa Luti.

اِنَّ اِبۡرٰهِيۡمَ لَحَلِيۡمٌ اَوَّاهٌ مُّنِيۡبٌ ﴿۷۵﴾

76. Kwa yakini Ibrahimu alikuwa mvumilivu sana, mpole sana (na) mwelekevu sana.

يٰۤاِبۡرٰهِيۡمُ اَعۡرِضۡ عَنۡ هٰذَا ۚ اِنَّهٗ قَدۡ جَآءَ اَمۡرُ رَبِّكَ ۚ وَاِنَّهُمۡ اٰتِيۡهِمۡ عَذَابٌ غَيۡرُ مَرۡدُوۡدٍ ﴿۷۶﴾

77. Ewe Ibrahimu, wacha haya. Kwa hakika amri ya Mola wako imekwisha fika, na hakika hao itawafikia adhabu isiyorudishwa.

Aya 73. Sio mradi wa Aya hii ya kwamba kushangaa kwa mke wa Nabii Ibrahimu ni kwa sababu alionea shaka habari aliyopewa na Allah. Mwanamke tu wa desturi hayuko tayari kufanyia shaka uwezo wa ajabu wa Allah, usiseme mke wa Nabii ambaye amekwisha ona Ishara nyingi za uwezo wa Allah. Kwa hakika alistaajabia habari ambayo si ya desturi ya kwamba atazaa mtoto na hali amekwisha kuwa mzee namna ile. Alistaajabia ukubwa wa zawadi aliyoahidiwa kupewa. Nabii Ibrahimu mwenyewe alionyesha kustaajabu kwa namna hiyo alipopewa habari ya kuzaa mtoto hali kisha kuwa mzee kabisa (tazama sura 15:55-57).

Aya 74. *Ahlal-Bait,* "Watu wa nyumba hii." Watu wa madhehebu fulani wanasema, wake wa Mtume *s.a.w.* si katika Ahlal-Bait zake, hali katika Aya hii neno hilo limetumiwa kwa ajili ya mke wa Nabii Ibrahimu, hali alikuwa hajazaa. Kwa hakika neno hili linapotumiwa katika Qur'an juu ya Nabii, basi linawakusanya na wakeze pia.

Aya 76. *Muniib.* Neno hili maana yake mtu anayegeukia kwa Allah mara kwa mara; mtu anayegeukia kwa Allah kwa kutubu; mtu anayemfanya mtu mwingine atoe mahali pake au pa mwingine (Akrab).

78. Na Wajumbe Wetu walipomfikia Luti, akawahuzunikia na akawa mnyonge kwa ajili yao, na akasema: Hii ni siku ngumu.

وَلَمَّا جَآءَتْ رُسُلُنَا لُوْطًا سِيْٓءَ بِهِمْ وَضَاقَ بِهِمْ ذَرْعًا وَّقَالَ هٰذَا يَوْمٌ عَصِيْبٌ ﴿٧٨﴾

79. Na kaumu yake wakamjia mbio wakimhamakia, na kabla ya haya walikuwa wakifanya maovu. Akasema; Enyi kaumu yangu, hao binti zangu (walioolewa katika nyumba zenu) hata kwa mtazamo wenu, ni watakatifu sana. Basi Mcheni Allah wala msinifedheheshe mbele ya wageni wangu. Je, miongoni mwenu hakuna hata mtu mwenye akili?

وَجَآءَهٗ قَوْمُهٗ يُهْرَعُوْنَ اِلَيْهِ ؕ وَمِنْ قَبْلُ كَانُوْا يَعْمَلُوْنَ السَّيِّاٰتِ ؕ قَالَ يٰقَوْمِ هٰٓؤُلَآءِ بَنَاتِيْ هُنَّ اَطْهَرُ لَكُمْ فَاتَّقُوا اللّٰهَ وَلَا تُخْزُوْنِ فِيْ ضَيْفِيْ ؕ اَلَيْسَ مِنْكُمْ رَجُلٌ رَّشِيْدٌ ﴿٧٩﴾

80. Wakasema: Bila shaka umekwisha jua sisi hatuna madai dhidi ya binti zako, na hakika unayajua tunayoyataka (kwamba uwafukuze hawa wageni).

قَالُوْا لَقَدْ عَلِمْتَ مَا لَنَا فِيْ بَنٰتِكَ مِنْ حَقٍّ ۚ وَاِنَّكَ لَتَعْلَمُ مَا نُرِيْدُ ﴿٨٠﴾

81. Akasema: Laiti ningalikuwa na nguvu kwenu, au nikajikinge kwenye nguzo yenye nguvu!

قَالَ لَوْ اَنَّ لِيْ بِكُمْ قُوَّةً اَوْ اٰوِيْٓ اِلٰى رُكْنٍ شَدِيْدٍ ﴿٨١﴾

Aya 78. *Lut.* Nabii Luti ambaye alikuwa katika wakati mmoja na Nabii Ibrahimu alikuwa babu wa watu wa Falastin (Palestine), Wamoab na Waammon. Baba yake aliitwa Haran bin Terah, hivyo Nabii Ibrahimu alikuwa amu wa Nabii Luti.

Aya 79. *Hao mabinti zangu.* Mradi wake ni kuwa watu hawana haja ya kuogopa kuwa yeye atapatana na wageni ili kuwaletea wao taabu, maana mabinti zake walikuwa wameolewa miongoni mwao; kama yeye ataleta udhia wangeweza kulipiza kisasi kwa kuwaadhibu mabinti zake. Hadithi zinazosimuliwa na watu kuwa Nabii Luti aliwatoa binti zake kwa watu hao ili wasimtie taabu ni za kusikitisha sana na hazistahili kukubaliwa kuwa ni jambo ambalo Mtume wa Mungu angeweza kulifanya .

Aya 80. Nabii Luti alipowaambia watu wa mji aliokaa kuwa binti zake wako mikononi mwao, na ya kwamba kama angefanya jambo lo lote la kuwaletea dhara basi wangejilipiza kisasi kwa binti zake. Nabii Luti namna hii aliwatoa binti zake kuwa dhamana. Sasa sheria katika nchi ile ilikuwa ya kwamba wanaume tu ndiyo hukubaliwa kwa dhamana. (Enc. Bri.). Hivyo watu walimwambia Luti ya kwamba hawatawafanya binti zake kuwa dhamana kwa kuwa ni kinyume na sheria ya nchi yao. Maneno haya, *Bila shaka umekwisha jua sisi hatuna haki juu ya binti zako,* yanaonyesha waziwazi watu wale hawakuja na nia ambayo baadhi ya wafasiri wanasema ya kwamba walikuwa nayo. Maneno haya, *Hakika unayajua tunayoyataka*, maana yake ni kuwa, "Unajua ya kwamba tusilotaka sasa ni kufika wageni hapa, basi kutuambia kuwa tuchukue dhamana na tuwaache wageni ni jambo tusiloweza kukubali."

قَالُوْا يٰلُوْطُ اِنَّا رُسُلُ رَبِّكَ لَنْ يَّصِلُوْٓا
اِلَيْكَ فَاَسْرِ بِاَهْلِكَ بِقِطْعٍ مِّنَ الَّيْلِ
وَلَا يَلْتَفِتْ مِنْكُمْ اَحَدٌ اِلَّا امْرَاَتَكَ ؕ
اِنَّهٗ مُصِيْبُهَا مَآ اَصَابَهُمْ ؕ اِنَّ
مَوْعِدَهُمُ الصُّبْحُ ؕ اَلَيْسَ الصُّبْحُ
بِقَرِيْبٍ ﴿٨١﴾

82. (Wale Wajumbe) wakasema: Ewe Luti, sisi ni Wajumbe wa Mola wako. Hawatakufikia kamwe. Kwa hiyo ondoka pamoja na watu wako wa nyumbani katika sehemu yo yote ya usiku, wala ye yote miongoni mwenu asitazame nyuma, isipokuwa mke wako. Hakika yeye utamfikia msiba utakaowafikia hao. Hakika miadi yao ni asubuhi. Je, asubuhi siyo karibu tu?

فَلَمَّا جَآءَ اَمْرُنَا جَعَلْنَا عَالِيَهَا سَافِلَهَا
وَاَمْطَرْنَا عَلَيْهَا حِجَارَةً مِّنْ سِجِّيْلٍ ۙ
مَّنْضُوْدٍ ﴿٨٢﴾

83. Basi ilipofika amri Yetu, Tukaupindua (mji ule) juu chini, na Tukawapigia, kwa mfululizo, hatua kwa hatua, mvua ya changarawe za udongo mgumu .

مُّسَوَّمَةً عِنْدَ رَبِّكَ ؕ وَمَا هِيَ مِنَ
الظّٰلِمِيْنَ بِبَعِيْدٍ ﴿٨٣﴾ ع

84. Zilizotiwa alama kwa Mola wako. Na (adhabu) hii haiko mbali na wadhalimu.

FUNGU 8

وَاِلٰى مَدْيَنَ اَخَاهُمْ شُعَيْبًا ؕ قَالَ يٰقَوْمِ
اعْبُدُوا اللّٰهَ مَا لَكُمْ مِّنْ اِلٰهٍ غَيْرُهٗ ؕ وَلَا
تَنْقُصُوا الْمِكْيَالَ وَالْمِيْزَانَ اِنِّيْٓ
اَرٰىكُمْ بِخَيْرٍ وَّاِنِّيْٓ اَخَافُ عَلَيْكُمْ
عَذَابَ يَوْمٍ مُّحِيْطٍ ﴿٨٤﴾

85. Na kwa Wamadiani (Tulimtuma) ndugu yao Shuaib. Akasema: Enyi watu wangu! Mwabuduni Allah, ninyi hamna Mungu ila Yeye; msipunguze kipimo wala mizani. Mimi nawaoneni katika hali njema, nami nawahofieni adhabu ya siku izungukayo.

Aya 81. *Nikajikinge kwenye nguzo yenye nguvu!* maana yake ni kwamba sasa sina la kufanya ila nijikinge kwa Allah na nimwombe ateremshe adhabu Yake juu yao.

Aya 82. Ushauri wa wajumbe wageni unaonyesha kwamba mazungumzo kati ya Luti na watu wake yaliendeshwa kwa faragha na kwamba hadi wakati huo hawakuwa na fursa ya moja kwa moja ya kumwona yeye au mtu mwingine ye yote katika nyumba hiyo. Baada ya kushindwa katika jaribio lao, wanaweza kuwa wamekusudia kumtembelea Luti kwa mara nyingine wakiwa wamejitayarisha vizuri zaidi kwa kuingia kwa nguvu katika nyumba hiyo. Jambo hili lilikanushwa wakati huo kwa ushauri wa wajumbe kuondoka katika nyumba hiyo pamoja na watu wote wa familia yake wakati wa usiku wa manane isipokuwa mkewe.

Aya 83. Inaonekana ya kuwa adhabu waliyopigwa nayo ni kupinduliwa na kufukiwa na tetemeko la nchi.

Aya 85. *Wamadiani.* Madian alikuwa mwana wa Nabii Ibrahimu aliyezaliwa na mkewe

وَيٰقَوْمِ اَوْفُوا الْمِكْيَالَ وَالْمِيْزَانَ
بِالْقِسْطِ وَلَا تَبْخَسُوا النَّاسَ اَشْيَآءَهُمْ
وَلَا تَعْثَوْا فِي الْاَرْضِ مُفْسِدِيْنَ ﴿٨٥﴾

86. Na enyi watu wangu timizeni kipimo na mizani kwa uadilifu wala msiwapunguzie watu vitu ambavyo kwa haki ni mali zao na msieneze uovu katika nchi mkifanya uharibifu.

بَقِيَّتُ اللّٰهِ خَيْرٌ لَّكُمْ اِنْ كُنْتُمْ
مُّؤْمِنِيْنَ ۚ وَمَآ اَنَا عَلَيْكُمْ بِحَفِيْظٍ ﴿٨٦﴾

87. (Mali) Aliyobakisha Allah ndiyo bora kwa ajili yenu, ikiwa ninyi mnaamini. Wala mimi si mhifadhi wenu.

قَالُوْا يٰشُعَيْبُ اَصَلٰوتُكَ تَاْمُرُكَ اَنْ
نَّتْرُكَ مَا يَعْبُدُ اٰبَآؤُنَآ اَوْ اَنْ نَّفْعَلَ فِيْٓ
اَمْوَالِنَا مَا نَشٰٓؤُا ۭ اِنَّكَ لَاَنْتَ الْحَلِيْمُ
الرَّشِيْدُ ﴿٨٧﴾

88. Wakasema: Ewe Shuaibu, je, Sala yako inakuamuru tuyaache waliyokuwa wakiyaabudu baba zetu, au tuache kufanya tupendavyo katika mali zetu? Bila shaka wewe ndiwe mpole sana, mwongofu.

قَالَ يٰقَوْمِ اَرَءَيْتُمْ اِنْ كُنْتُ عَلٰي بَيِّنَةٍ
مِّنْ رَّبِّيْ وَرَزَقَنِيْ مِنْهُ رِزْقًا حَسَنًا ۭ وَمَآ
اُرِيْدُ اَنْ اُخَالِفَكُمْ اِلٰي مَآ اَنْهٰىكُمْ
عَنْهُ ۭ اِنْ اُرِيْدُ اِلَّا الْاِصْلَاحَ مَا
اسْتَطَعْتُ ۭ وَمَا تَوْفِيْقِيْٓ اِلَّا بِاللّٰهِ ۭ
عَلَيْهِ تَوَكَّلْتُ وَاِلَيْهِ اُنِيْبُ ﴿٨٨﴾

89. Akasema: Enyi watu wangu, mwaonaje kama ninayo dalili wazi itokayo kwa Mola wangu, na Ameniruzuku riziki njema kutoka Kwake? Wala sipendi kupinzana nanyi kwa kufanya yale ninayowakatazeni. Sitaki ila kusuluhisha ninavyoweza. Na sipati uwezo ila kwa Allah. Kwake ninategemea, na Kwake naelekea.

Katura (Mwanzo 25:1-2). Dhuria zake waliitwa Madiani kwa kufuata desturi ya kizamani. Au inaweza kuwa ya kwamba asili yao waliitwa "Banu Madian" (watoto wa Madiani), lakini baadaye maneno haya yakafupishwa na kuwa Madiani. Mji mkuu wa watu hawa pia uliitwa Madiani, ambao unaweza kuwa kifupisho cha *Duuri Madiani* (nyumba za Madiani). Mji huu ulikuwa penye Ghuba ya 'Akaba, pwani ya Bara Arabu, penye umbali wa maili sita au saba kutoka baharini. Misafara ya biashara iliyokuwa ikienda Misri kutoka Bara Arabu ilipita katika mji huo. Hivi sasa kuna miji midogo midogo inayoitwa Madiani, lakini mji wenyewe wa asili sasa haupo. Watoto wa Madiani waliishi kaskazini ya Hijazi na ni wao waliojenga mji huo. Mji huo ndiko alikokimbilia Nabii Musa wakati Firauni na mawaziri wake walipotaka kumwua; na pia ni ujiranini mwa mji huo walikokaa Nabii Musa pamoja na Waisraeli baada ya kuivuka Bahari ya Sham.

Habari za Nabii *Shuaib* tazama sura 7:86.

وَيٰقَوْمِ لَا يَجْرِمَنَّكُمْ شِقَاقِيْٓ اَنْ
يُّصِيْبَكُمْ مِّثْلُ مَآ اَصَابَ قَوْمَ نُوْحٍ اَوْ
قَوْمَ هُوْدٍ اَوْ قَوْمَ صٰلِحٍ ؕ وَمَا قَوْمُ لُوْطٍ
مِّنْكُمْ بِبَعِيْدٍ ﴿٨٩﴾

90. Na enyi watu wangu! kuniadui kusiwaelekezeni kwenye jambo lile litakalowafanya yawasibuni kama yaliyowasibu watu wa Nuhu au watu wa Hudi au watu wa Saleh, na watu wa Luti hawako mbali nanyi.

وَاسْتَغْفِرُوْا رَبَّكُمْ ثُمَّ تُوْبُوْٓا اِلَيْهِ ؕ اِنَّ
رَبِّيْ رَحِيْمٌ وَّدُوْدٌ ﴿٩٠﴾

91. Na ombeni msamaha kwa Mola wenu, kisha tubuni Kwake. Hakika Mola wangu ni Mrehemevu, Apendaye sana.

قَالُوْا يٰشُعَيْبُ مَا نَفْقَهُ كَثِيْرًا مِّمَّا
تَقُوْلُ وَاِنَّا لَنَرٰىكَ فِيْنَا ضَعِيْفًا ۚ وَلَوْلَا
رَهْطُكَ لَرَجَمْنٰكَ ۖ وَمَآ اَنْتَ عَلَيْنَا
بِعَزِيْزٍ ﴿٩١﴾

92. Wakasema: Ewe Shuaibu, hatufahamu mengi ya hayo uyasemayo, na bila shaka sisi tunakuona u mdhaifu kati yetu. Na kama si kabila yako, bila shaka tungekupiga mawe, wala wewe huna mamlaka juu yetu.

قَالَ يٰقَوْمِ اَرَهْطِيْٓ اَعَزُّ عَلَيْكُمْ مِّنَ
اللّٰهِ ؕ وَاتَّخَذْتُمُوْهُ وَرَآءَكُمْ ظِهْرِيًّا ؕ
اِنَّ رَبِّيْ بِمَا تَعْمَلُوْنَ مُحِيْطٌ ﴿٩٢﴾

93. Akasema: Enyi watu wangu! je, kabila yangu ina nguvu zaidi kwenu kuliko Allah? Na mmemfanya Yeye kuwa nyuma ya migongo yenu. Hakika Mola wangu anayazunguka mnayoyatenda.

Aya 90. Aya hii inaonyesha ya kwamba Shuaibu alifika baada ya Nuhu, Hudi Saleh na Luti (na hivyo baada ya Ibrahimu pia), lakini alikuwako kabla ya wakati wa Musa, ingawa Musa pamoja na watu wake walikaa katika ardhi ya watu wa Shuaibu.

Aya 91. Mara kwa mara inasemwa na maadui wa Uislamu ya kwamba Uislamu unasaidia dhambi kudumu kwa kuacha wazi mlango wa toba. Ubishi huu unaletwa kwa sababu ya kutofahamu tauba ya Kiislamu ni nini. Tauba (toba) siyo kutamka neno "Nasikitika" au "Natubu" kisha kudhani ya kuwa dhambi zitasamehewa. Hii siyo maana ya toba ya Kiislamu. Islam haikubali ya kwamba mtu anaweza kutoka katika ubaya na kuingia katika wema, au kutoka katika daraja la chini la wema kwenda daraja la juu la wema kwa kuchupa mara moja. Mabadiliko hayo yanafikiwa kwa kupitia madaraja mengi. Mtu mwenye dhambi anapoelekea kwa Allah anaanza kwa kujichungua hali ya moyo wake na anaanza kuona haya na kujuta, na matokeo yake yanakuwa anafanya bidii kujikinga kwa Allah. Hili ndilo daraja la *istighfaar.* Kisha linakuja daraja la *isti'aadha*, yaana kumwomba Mungu akulinde na matokeo mabaya ya matendo mabaya unayoyajutia. Mwisho linakuja daraja la *tauba* (toba), yaani kumgeukia Allah na kumpenda kwa moyo wote na kwa roho yote na kujiunganisha naye mwungano wa kweli. Hivyo, toba inayofundishwa na dini ya Kiislamu ndiyo njia hasa ya kumpatia mtu utakaso na kumrejesha kwa Mola wake mtu aliyepotea. Mtu aliyekosa akijua kuwa hatasamehewa hata afanye bidii ya namna gani, basi nini tena kitamzuia kuendelea na anasa za maisha maovu?

94. Na enyi watu wangu! fanyeni mwezavyo, mimi pia ninafanya. Hivi karibuni mtajua ni nani itakayemfikia adhabu ifedheheshayo na ni nani aliye mwongo. Na ngojeni, mimi pia ninangoja pamoja nanyi.

وَيٰقَوْمِ اعْمَلُوْا عَلٰى مَكَانَتِكُمْ اِنِّيْ
عَامِلٌ ؕ سَوْفَ تَعْلَمُوْنَ ۙ مَنْ يَّاْتِيْهِ
عَذَابٌ يُّخْزِيْهِ وَمَنْ هُوَ كَاذِبٌ ؕ
وَارْتَقِبُوْٓا اِنِّيْ مَعَكُمْ رَقِيْبٌ ﴿٩٤﴾

95. Na ilipofika amri Yetu, Tukamwokoa Shuaibu na wale walioamini pamoja naye kwa rehema Yetu, na wale waliodhulumu adhabu ikawashika, na wakawa majumbani mwao wameanguka kifudifudi.

وَلَمَّا جَآءَ اَمْرُنَا نَجَّيْنَا شُعَيْبًا وَّالَّذِيْنَ
اٰمَنُوْا مَعَهٗ بِرَحْمَةٍ مِّنَّا وَاَخَذَتِ الَّذِيْنَ
ظَلَمُوا الصَّيْحَةُ فَاَصْبَحُوْا فِيْ دِيَارِهِمْ
جٰثِمِيْنَ ﴿٩٥﴾

96. Kana kwamba hawakuwamo humo. Sikilizeni! Wameangamia Wamadiani kama walivyoangamia Wathamudi. ع ٨

كَاَنْ لَّمْ يَغْنَوْا فِيْهَا ؕ اَلَا بُعْدًا لِّمَدْيَنَ
كَمَا بَعِدَتْ ثَمُوْدُ ﴿٩٦﴾

FUNGU 9

97. Na kwa yakini Tulimtuma Musa pamoja na Ishara Zetu na mamlaka yaliyo wazi.

وَلَقَدْ اَرْسَلْنَا مُوْسٰى بِاٰيٰتِنَا وَسُلْطٰنٍ
مُّبِيْنٍ ﴿٩٧﴾

98. Kwa Firauni na wakuu wake. Lakini wao walifuata amri ya Firauni, na amri ya Firauni haikuwa sawa.

اِلٰى فِرْعَوْنَ وَمَلَا۟ئِهٖ فَاتَّبَعُوْٓا اَمْرَ
فِرْعَوْنَ ۚ وَمَآ اَمْرُ فِرْعَوْنَ بِرَشِيْدٍ ﴿٩٨﴾

99. Atawatangulia watu wake siku ya Kiyama na atawaongoza hadi kwenye shimo la Moto. Ni pabaya palioje mahali hapo panapofikiwa.

يَقْدُمُ قَوْمَهٗ يَوْمَ الْقِيٰمَةِ فَاَوْرَدَهُمُ
النَّارَ ؕ وَبِئْسَ الْوِرْدُ الْمَوْرُوْدُ ﴿٩٩﴾

Aya 93. Manabii wanakuwa na ghera juu ya Allah, hivyo Shuaibu anawalaumu watu wake ya kwamba badala ya kumwogopa Mungu wao wanawaogopa zaidi watu wa kabila yake. Kadhalika Mtume *s.a.w.* hakukosa kuonyesha mapenzi yake na ghera yake kwa ajili ya Allah. Katika vita vya Uhud, maadui walipodhani kuwa wamemwua Mtume *s.a.w.* wakaanza kupiga shangwe wakitukuza sanamu lao, Hubal. Ingawa Mtume *s.a.w* na wafuasi wake wachache walikuwa katika hatari sana, lakini Mtume akawakaripia Waislamu kwa nini hawakuwajibu. Akawaambia wainue sana sauti kumtukuza Allah.

وَ اُتْبِعُوْا فِيْ هٰذِهٖ لَعْنَةً وَّ يَوْمَ الْقِيٰمَةِ ؕ
بِئْسَ الرِّفْدُ الْمَرْفُوْدُ ﴿۹۹﴾

100. Na wamefuatishiwa laana katika hii (dunia) na (pia) Siku ya Kiyama. Ni mbaya iliyoje zawadi itakayotolewa.

ذٰلِكَ مِنْ اَنْۢبَآءِ الْقُرٰى نَقُصُّهٗ عَلَيْكَ مِنْهَا
قَآئِمٌ وَّ حَصِيْدٌ ﴿۱۰۰﴾

101. Hizo ni katika habari za miji Tunayokusimulia. Baadhi yao ipo na (mingine) imefutwa.

وَ مَا ظَلَمْنٰهُمْ وَ لٰكِنْ ظَلَمُوْۤا اَنْفُسَهُمْ
فَمَاۤ اَغْنَتْ عَنْهُمْ اٰلِهَتُهُمُ الَّتِيْ يَدْعُوْنَ
مِنْ دُوْنِ اللّٰهِ مِنْ شَيْءٍ لَّمَّا جَآءَ اَمْرُ
رَبِّكَ ؕ وَ مَا زَادُوْهُمْ غَيْرَ تَتْبِيْبٍ ﴿۱۰۱﴾

102. Nasi Hatukuwadhulumu, walakini wao wamejidhulumu wenyewe; na waungu wao waliokuwa wakiwaita badala ya Allah hawakuwafaa kitu ilipofika amri ya Mola wako, nao hawakuwazidishia ila maangamizo.

وَ كَذٰلِكَ اَخْذُ رَبِّكَ اِذَاۤ اَخَذَ الْقُرٰى
وَ هِيَ ظَالِمَةٌ ؕ اِنَّ اَخْذَهٗۤ اَلِيْمٌ شَدِيْدٌ ﴿۱۰۲﴾

103. Na hivi ndivyo lilivyo shiko la Mola wako Anapoishika miji hali ikidhulumu. Hakika shiko Lake laumiza (na) kali.

اِنَّ فِيْ ذٰلِكَ لَاٰيَةً لِّمَنْ خَافَ عَذَابَ
الْاٰخِرَةِ ؕ ذٰلِكَ يَوْمٌ مَّجْمُوْعٌ ۙ لَّهُ
النَّاسُ وَ ذٰلِكَ يَوْمٌ مَّشْهُوْدٌ ﴿۱۰۳﴾

104. Kwa yakini katika hilo imo Ishara kwa yule aogopaye adhabu ya Akhera. Hiyo ndiyo Siku itakayokusanywa watu, na hiyo ndiyo siku itakayoshuhudiwa.

وَ مَا نُؤَخِّرُهٗۤ اِلَّا لِاَجَلٍ مَّعْدُوْدٍ ﴿۱۰۴﴾

105. Na Hatuiahirishi ila kwa muda unaohesabiwa.

يَوْمَ يَاْتِ لَا تَكَلَّمُ نَفْسٌ اِلَّا بِاِذْنِهٖ ۚ
فَمِنْهُمْ شَقِيٌّ وَّ سَعِيْدٌ ﴿۱۰۵﴾

106. Siku itakapofika, mtu ye yote hatasema ila kwa ruhusa Yake; basi baadhi yao watakuwa wenye bahati mbaya na (wengine) wenye bahati nzuri.

فَاَمَّا الَّذِيْنَ شَقُوْا فَفِي النَّارِ لَهُمْ فِيْهَا
زَفِيْرٌ وَّ شَهِيْقٌ ﴿۱۰۶﴾

107. Na ama wale wenye bahati mbaya, basi (wao watatiwa) Motoni, humo watapiga kite na kutoa kwikwi.

خٰلِدِيْنَ فِيْهَا مَا دَامَتِ السَّمٰوٰتُ
وَ الْاَرْضُ اِلَّا مَا شَآءَ رَبُّكَ ؕ اِنَّ رَبَّكَ
فَعَّالٌ لِّمَا يُرِيْدُ ﴿۱۰۷﴾

108. Watakaa humo maadamu mbingu na ardhi vinadumu, isipokuwa Apendavyo Mola wako. Hakika Mola wako Hufanya Apendavyo.

109. Na ama wale wenye bahati njema, basi wao (wataingizwa) Peponi; watakaa humo maadamu mbingu na ardhi vinadumu, isipokuwa Apendavyo Mola wako - ni kipawa kisichokatizwa.

110. Basi (ewe msikiaji) usiwe na shaka juu ya wanayoyaabudu hao. Hawaabudu isipokuwa kama walivyoabudu baba zao zamani; na bila shaka sisi Tutawapa sehemu yao sawasawa bila kupunguzwa.

وَاَمَّا الَّذِيْنَ سُعِدُوْا فَفِى الْجَنَّةِ خٰلِدِيْنَ
فِيْهَا مَا دَامَتِ السَّمٰوٰتُ وَالْاَرْضُ اِلَّا
مَا شَآءَ رَبُّكَ ؕ عَطَآءً غَيْرَ مَجْذُوْذٍ ﴿۱۰۸﴾
فَلَا تَكُ فِىْ مِرْيَةٍ مِّمَّا يَعْبُدُ هٰٓؤُلَآءِ ؕ
مَا يَعْبُدُوْنَ اِلَّا كَمَا يَعْبُدُ اٰبَآؤُهُمْ
مِّنْ قَبْلُ ؕ وَاِنَّا لَمُوَفُّوْهُمْ نَصِيْبَهُمْ
غَيْرَ مَنْقُوْصٍ ﴿۱۰۹﴾ ع

Aya 109. Aya hii na iliyotangulia inabainisha jambo kubwa ambalo dini ya Kiislamu inahitilafiana na dini nyinginezo, yaani jambo la kuokoka.

Dini ya Kibaniani inafundisha ya kwamba Pepo na Jahanamu vyote viwili vina mwisho, na mtu aliyetiwamo baadaye atarudishwa hapa duniani.

Dini ya Kiyahudi inafundisha ya kuwa watakaoingia Peponi ni Mayahudi tu, na kama Myahudi ye yote atatiwa Motoni, basi hatakaa humo zaidi kuliko miezi 11; na wasio Mayahudi wataungua humo milele.

Wakristo wanasadiki ya kwamba Pepo na Jahanamu vyote viwili ni vya milele ingawa baadhi ya madhehebu zao wanasadiki ya kwamba mwishoni Pepo itakoma.

Lakini Islam inafundisha ya kwamba Pepo ni ya milele na Jahanamu ndiyo yenye kikomo. Kwa mfano katika Aya hii Pepo imesemwa *ni kipawa kisichokatizwa;* lakini Jahanamu haikusemwa hivyo. Basi ni wazi ya kuwa Pepo haina mwisho na Jahanamu ina ukomo.

Abu Said Khudri anasimulia hadithi ndefu ya Mtume *s.a.w.* inayoonyesha waziwazi ya kuwa Jahanamu ina mwisho. Mtume *s.a.w.* alisema ya Kwamba: "Siku ya Kiyama Allah atawapa ruhusa watu fulani wenye vyeo vya juu kuwaombea wenye dhambi. Mwishoni waaminio wa kawaida watapewa ruhusa kuwaombea watu. Kwanza watawaombea wale wanaowajua. Kisha, kwa amri ya Allah watawaombea wakosefu waliobakiwa na imani kidogo mioyoni mwao; hata mwishowe watawaombea wale wenye imani ndogo sawa na punje katika mioyo yao. Hapo hawatabakia katika Jahanamu isipokuwa wale tu ambao hawakufanya wema wo wote. Kisha Allah atasema, "Malaika wamekwisha waombea watu, na Manabii na waaminio wamekwisha waombea, na sasa ni zamu yangu Mimi Ambaye ni Mrehemevu wa warehemevu." Kisha Allah atatwaa gao la watu toka Jahanamu na kuwatoa hata hao ambao hawakufanya wema wo wote" (Bukhari na Muslim).

Ni wazi gao la Mungu haliwezi kubakisha hata mtu mmoja katika Jahanamu.

Tena Mtume *s.a.w.* alisema. "Utafika wakati juu ya Jahanamu malango yake yatakapogongana na hatakuwamo humo ye yote. Hayo ni baada ya kuwa wamekaa humo kwa karne nyingi" (Musnad).

Hadithi hiyo ya juu ambayo ilisimuliwa na Abdalla bin 'Amri, pia imesimuliwa na Abu Hureira. Jabir, Abu Said Khudri na Abdullah bin Umar nao wamesemwa walisema usemi kama huo (Fat'h).

Katika sura 11:120 Allah amesema kuwa amewaumba watu ili apate kuwarehemu, wanavyokubali tafsiri hiyo wanazuoni wakubwa kama Ibni Abbas, Taa'uus, Mujahid, Dhahhaak, Katada na Ikrima (Kathir, Manthur na Tahawi). Hivyo kama mtu atakaa Motoni milele, atarehemewa lini? Basi ni lazima Moto uwe na kikomo.

Katika Qur'an mna Aya zinazoonyesha wazi ya kuwa Jahanamu ni kitu cha kupita ingawa watakaotiwa ndani yake wataadhibiwa kwa miaka mingi sana, hata ni kama milele kwa kupimia

FUNGU 10

وَلَقَدْ اٰتَيْنَا مُوْسَى الْكِتٰبَ فَاخْتُلِفَ فِيْهِ ؕ وَلَوْلَا كَلِمَةٌ سَبَقَتْ مِنْ رَّبِّكَ لَقُضِيَ بَيْنَهُمْ ؕ وَاِنَّهُمْ لَفِيْ شَكٍّ مِّنْهُ مُرِيْبٍ ﴿١١١﴾

111. Na kwa yakini Tulimpa Musa Kitabu, lakini zikatiwa hitilafu ndani yake; na kama si neno lililotangulia kutoka kwa Mola wako, bila shaka ingalihukumiwa kati yao; na hakika wao wamo katika shaka ihangaishayo juu yake.

وَاِنَّ كُلًّا لَّمَّا لَيُوَفِّيَنَّهُمْ رَبُّكَ اَعْمَالَهُمْ ؕ اِنَّهٗ بِمَا يَعْمَلُوْنَ خَبِيْرٌ ﴿١١٢﴾

112. Na hakika Mola wako Atawapa hao wote malipo ya vitendo vyao sawasawa. Bila shaka Yeye Anazo habari za wanayoyatenda.

فَاسْتَقِمْ كَمَاۤ اُمِرْتَ وَمَنْ تَابَ مَعَكَ وَلَا تَطْغَوْا ؕ اِنَّهٗ بِمَا تَعْمَلُوْنَ بَصِيْرٌ ﴿١١٣﴾

113. Basi, endelea kama ulivyoamuriwa wewe na yule anayeelekea (kwa Mungu) pamoja nawe; wala msiruke mipaka (enyi waaminio). Hakika Yeye Anayaona mnayoyatenda.

وَلَا تَرْكَنُوْۤا اِلَى الَّذِيْنَ ظَلَمُوْا فَتَمَسَّكُمُ النَّارُ ۙ وَمَا لَكُمْ مِّنْ دُوْنِ اللّٰهِ مِنْ اَوْلِيَآءَ ثُمَّ لَا تُنْصَرُوْنَ ﴿١١٤﴾

114. Wala msielekee kwa wale waliodhulumu usije ukawaguseni Moto. Na hamtakuwa na mlinzi badala ya Allah; kisha ninyi hamtasaidiwa.

وَاَقِمِ الصَّلٰوةَ طَرَفَيِ النَّهَارِ وَزُلَفًا مِّنَ الَّيْلِ ؕ اِنَّ الْحَسَنٰتِ يُذْهِبْنَ السَّيِّاٰتِ ؕ ذٰلِكَ ذِكْرٰى لِلذّٰكِرِيْنَ ﴿١١٥﴾ۚ

115. Na simamisha Sala katika sehemu mbili za mchana na nyakati za usiku (zilizo karibu na mchana). Hakika mema huyaondoa maovu. Huo ndio ukumbusho kwa wakumbukao.

وَاصْبِرْ فَاِنَّ اللّٰهَ لَا يُضِيْعُ اَجْرَ الْمُحْسِنِيْنَ ﴿١١٦﴾

116. Na subiri, kwani hakika Allah Hapotezi ujira wa wafanyao mema.

---

kwa kibinadamu, na mwisho watatoka ili wakapate rehema za Mungu na kutiwa Peponi. Rai hii ndiyo aliyokuwa nayo Ibni Mas'ud na Abu Hureira. Na Ibni Taimiyya ameeleza ya kuwa Seyidna Umar, Ibni Abbas, Anas na mufasirina wengi wanashika rai hiyo.

Aya 113. Athari kubwa aliyopata Mtume *s.a.w.* kwa Aya hii inaonekana kwa maneno asemayo: "Sura *Huud* na sura zenzie zimenifanya mzee kabla ya wakati wangu" (Manthur). Abu Ali Sirri anasimuliwa kusema ya kwamba siku moja alimwona Mtume *s.a.w.* katika ndoto na

فَلَوْلَا كَانَ مِنَ الْقُرُوْنِ مِنْ قَبْلِكُمْ اُولُوْا
بَقِيَّةٍ يَّنْهَوْنَ عَنِ الْفَسَادِ فِي الْاَرْضِ اِلَّا
قَلِيْلًا مِّمَّنْ اَنْجَيْنَا مِنْهُمْ ۚ وَاتَّبَعَ الَّذِيْنَ
ظَلَمُوْا مَآ اُتْرِفُوْا فِيْهِ وَكَانُوْا
مُجْرِمِيْنَ ﴿١١٧﴾

117. Basi mbona hawakuwamo katika vizazi vya kabla yenu watu wenye akili, wenye kukataza uharibifu katika nchi isipokuwa wachache Tuliowaokoa miongoni mwao? Na wale waliodhulumu walifuata waliyostareheshwa nayo na wakawa wakosefu.

وَمَا كَانَ رَبُّكَ لِيُهْلِكَ الْقُرٰى بِظُلْمٍ
وَّاَهْلُهَا مُصْلِحُوْنَ ﴿١١٨﴾

118. Na Mola wako si wa kuiangamiza miji kwa dhuluma na hali watu wake ni watendao mema.

وَلَوْ شَآءَ رَبُّكَ لَجَعَلَ النَّاسَ اُمَّةً
وَّاحِدَةً وَّلَا يَزَالُوْنَ مُخْتَلِفِيْنَ ﴿١١٩﴾

119. Na kama Mola wako Angalipenda, bila shaka Angaliwafanya watu kuwa umati mmoja. Nao wataendelea kuhitilafiana.

اِلَّا مَنْ رَّحِمَ رَبُّكَ ؕ وَلِذٰلِكَ خَلَقَهُمْ ؕ
وَتَمَّتْ كَلِمَةُ رَبِّكَ لَاَمْلَـَٔنَّ جَهَنَّمَ
مِنَ الْجِنَّةِ وَالنَّاسِ اَجْمَعِيْنَ ﴿١٢٠﴾

120. Isipokuwa yule ambaye Mola wako Amemrehemu; na kwa (rehema) hiyo Amewakhuluku. Na litatimia neno la Mola wako: Kwa kweli Nitaijaza Jahanamu kwa majinni na watu wote.

وَكُلًّا نَّقُصُّ عَلَيْكَ مِنْ اَنْۢبَآءِ الرُّسُلِ مَا
نُثَبِّتُ بِهٖ فُؤَادَكَ ۚ وَجَآءَكَ فِيْ هٰذِهِ
الْحَقُّ وَمَوْعِظَةٌ وَّذِكْرٰى لِلْمُؤْمِنِيْنَ ﴿١٢١﴾

121. Na Tunakusimulia yote katika habari za Mitume ambazo Tunauthibitisha moyo wako. Na katika haya imekufikia haki na mawaidha na ukumbusho kwa waaminio.

وَقُلْ لِّلَّذِيْنَ لَا يُؤْمِنُوْنَ اعْمَلُوْا عَلٰى
مَكَانَتِكُمْ ؕ اِنَّا عٰمِلُوْنَ ﴿١٢٢﴾
وَانْتَظِرُوْا ۚ اِنَّا مُنْتَظِرُوْنَ ﴿١٢٣﴾

122. Na waambie wale wasioamini: Fanyeni mnavyoweza mahali penu, nasi pia tunafanya.

123. Na ngojeni, hakika sisi tunangoja.

---

akamwuliza kama ni kweli alipata kusema kuwa sura *Huud* imemfanya mzee. Mtume s.a.w. akakubali kuwa alisema. Hapo Abu Ali akauliza tena kama ni habari za Manabii na kuangamizwa kwa watu wao kulikomfanya mzee. Mtume *s.a.w.* akajibu: "La, bali maneno haya, *Basi (ewe Mtume), endelea kama ulivyoamuriwa* yamenifanya hivyo" (Bukhari).

124. Na siri za mbingu na ardhi ni za Allah, na habari yote itarudishwa Kwake. Basi Mwabudu Yeye na kumtegemea. Na Mola wako Haghafiliki na yale mnayoyatenda.

وَلِلّٰهِ غَيْبُ السَّمٰوٰتِ وَالْاَرْضِ وَاِلَيْهِ يُرْجَعُ الْاَمْرُ كُلُّهٗ فَاعْبُدْهُ وَتَوَكَّلْ عَلَيْهِ ؕ وَمَا رَبُّكَ بِغَافِلٍ عَمَّا تَعْمَلُوْنَ ﴿۱۲۳﴾

Aya 124. Aya hii ambayo inamalizia sura hii ina maana ya kwamba bishara kubwa zilizobashiriwa katika sura hii juu ya ushindi wa dini ya Kiislamu na kushindwa kwa makafiri zinaonekana kama haiwezekani zitimie hivi sasa, lakini hakuna jambo lisilowezekana kwa Allah, na bishara hizi karibuni zitakuja timia.

Maneno haya, *Basi Mwabudu Yeye,* yanawakumbusha waaminio ya kwamba ingawa ahadi za Allah za kushinda kwa Uislamu zimetolewa, lakini wakumbuke ya kuwa Allah ni Mungu Mwivu, na upungufu wao na makosa yao yanaweza kukawiza ahadi hizo zisitimizwe upesi. Hivyo wakazane kumwabudu Allah na pia wamtegemee Yeye tu.

سُوْرَةُ يُوْسُفَ مَكِّيَّةٌ وَّ هِيَ مَعَ الْبَسْمَلَةِ مِائَةٌ وَّاثْنَتَا عَشْرَةَ اٰيَةً وَّ اثْنَا عَشَرَ رُكُوْعًا

12. SURA YUUSUF

Imeteremshwa Makka

Ina mafungu 12 na Aya 112 pamoja na Bismilahi

بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ ①

1. Kwa jina la Allah, Mwingi wa rehema, Mwingi wa ukarimu.

الٓرٰ ۚ تِلْكَ اٰيٰتُ الْكِتٰبِ الْمُبِيْنِ ②

2. Mimi ndiye Allah Nionaye. Hizi ni Aya za Kitabu kielezacho.

اِنَّاۤ اَنْزَلْنٰهُ قُرْءٰنًا عَرَبِيًّا لَّعَلَّكُمْ تَعْقِلُوْنَ ③

3. Hakika Sisi Tumeiteremsha hiyo Qur'an (Kitabu kisomwacho mara kwa mara), kwa Kiarabu (lugha fasaha iliyo bayana) ili mpate kufahamu.

نَحْنُ نَقُصُّ عَلَيْكَ اَحْسَنَ الْقَصَصِ بِمَاۤ اَوْحَيْنَاۤ اِلَيْكَ هٰذَا الْقُرْاٰنَ ۖ وَاِنْ كُنْتَ مِنْ قَبْلِهٖ لَمِنَ الْغٰفِلِيْنَ ④

4. Sisi Tunakusimulia kwa simulizi nzuri kwa kukufunulia Qur'an hii, ingawa ulikuwa kabla ya haya miongoni mwa wasio na habari.

اِذْ قَالَ يُوْسُفُ لِاَبِيْهِ يٰۤاَبَتِ اِنِّيْ رَاَيْتُ اَحَدَ عَشَرَ كَوْكَبًا وَّ الشَّمْسَ وَالْقَمَرَ رَاَيْتُهُمْ لِيْ سٰجِدِيْنَ ⑤

5. (Kumbuka) Yusuf alipomwambia baba yake: Ewe Babaangu, hakika nimeona (katika ndoto) nyota kumi na moja na jua na mwezi, nimeviona vikinisujudia.

Masahaba wengi zaidi wanakubali ya kuwa sura hii nzima ilishuka Makka; lakini Ibni Abbas na Katada wanasema ya kuwa Aya 2 mpaka 4 zilishuka baada ya Mtume kuhamia Madina.

Sura hii ina jambo moja la namna ya peke yake. Yote nzima inaeleza habari za maisha ya Mtume mmoja tu - Yusuf. Sababu yake ni kuwa maisha ya Nabii Yusuf yanafanana sana na maisha ya Mtume s.a.w. hata katika mambo madogo madogo. Na hii yote imekuwa hivi ili kuwaonya watu ya kuwa mambo yatatokea kwa Mtume *s.a.w.* kama vile yalivyotokea kwa Nabii Yusuf.

Aya 2. *Alif Laam Raa,* "Mimi ndiye Allah Nionaye." Sifa ya Allah ya kuona inayorejewa katika kifungu hiki cha maneno inakusudiwa kuwavuta wasioamini watumie vipawa vyao vya kuona. Sura hii inawaambia wasioamini ya kwamba Mtume *s.a.w.* anafanana sana na Nabii Yusuf, na ya kwamba si haki kwao kumkadhibisha kabla hawajaona mwisho wake.

Aya 3. *Qur'aanan 'arabiyyan,* "Qur'an kwa Kiarabu." Maneno haya katika Kiarabu yana maana hizi: (1) Inayosomwa sana na mfululizo; (2) inayoweza kueleza maana yake kwa njia iliyo wazi, fasaha na ya kutosheleza (Akrab na Lane).

Aya 5. Yusuf alikuwa mtoto wa kiume wa kumi na moja katika watoto kumi na mbili wa Nabii Yakubu ambaye anaitwa pia Israeli.

قَالَ يٰبُنَيَّ لَا تَقْصُصْ رُءْيَاكَ عَلٰٓى
اِخْوَتِكَ فَيَكِيْدُوْا لَكَ كَيْدًا ؕ اِنَّ
الشَّيْطٰنَ لِلْاِنْسَانِ عَدُوٌّ مُّبِيْنٌ ۝٥

6. Akasema: Ewe mwanangu! usisimulie ndoto yako kwa ndugu zako, wasije wakakufanyia hila. Hakika Shetani kwa mwanadamu ni adui dhahiri.

وَكَذٰلِكَ يَجْتَبِيْكَ رَبُّكَ وَيُعَلِّمُكَ مِنْ
تَاْوِيْلِ الْاَحَادِيْثِ وَيُتِمُّ نِعْمَتَهٗ عَلَيْكَ
وَعَلٰٓى اٰلِ يَعْقُوْبَ كَمَآ اَتَمَّهَا عَلٰٓى اَبَوَيْكَ
مِنْ قَبْلُ اِبْرٰهِيْمَ وَاِسْحٰقَ ؕ اِنَّ رَبَّكَ
عَلِيْمٌ حَكِيْمٌ ۝٦ ع

7. Na hivyo Mola wako Atakuchagua na kukufundisha hakika ya mambo na kutimiza neema Yake juu yako na juu ya watoto wa Yakubu kama Alivyotimiza zamani juu ya baba zako, Ibrahimu na Isihaka. Bila shaka Mola wako ni Mjuzi, Mwenye hekima.

FUNGU 2

لَقَدْ كَانَ فِيْ يُوْسُفَ وَاِخْوَتِهٖٓ اٰيٰتٌ
لِّلسَّآئِلِيْنَ ۝٧

8. Kwa yakini katika Yusuf na ndugu zake ziko Ishara kwa waulizao.

اِذْ قَالُوْا لَيُوْسُفُ وَاَخُوْهُ اَحَبُّ اِلٰٓى
اَبِيْنَا مِنَّا وَنَحْنُ عُصْبَةٌ ؕ اِنَّ اَبَانَا لَفِيْ
ضَلٰلٍ مُّبِيْنٍ ۝٨

9. (Kumbuka) waliposema: Hakika Yusuf na nduguye wanapendwa zaidi na baba yetu kuliko sisi, hali sisi ni kundi lenye nguvu. Hakika baba yetu yumo katika upotevu dhahiri.

اقْتُلُوْا يُوْسُفَ اَوِ اطْرَحُوْهُ اَرْضًا يَّخْلُ
لَكُمْ وَجْهُ اَبِيْكُمْ وَتَكُوْنُوْا مِنْۢ بَعْدِهٖ
قَوْمًا صٰلِحِيْنَ ۝٩

10. Mwueni Yusuf au mtupeni nchi (za mbali), ili uso wa baba yenu uwaelekeeni, na baada ya haya mtakuwa watu wema.

قَالَ قَآئِلٌ مِّنْهُمْ لَا تَقْتُلُوْا يُوْسُفَ
وَاَلْقُوْهُ فِيْ غَيٰبَتِ الْجُبِّ يَلْتَقِطْهُ
بَعْضُ السَّيَّارَةِ اِنْ كُنْتُمْ فٰعِلِيْنَ ۝١٠

11. Akasema msemaji kati yao: Msimwue Yusuf, lakini mtupeni katika shimo la kisima kirefu, watamwokota baadhi ya wasafiri, kama ninyi ni wafanyao (jambo).

قَالُوْا يٰٓاَبَانَا مَا لَكَ لَا تَاْمَنَّا عَلٰى يُوْسُفَ
وَاِنَّا لَهٗ لَنٰصِحُوْنَ ۝١١

12. Wakasema: Ewe baba yetu, mbona hutuamini juu ya Yusuf na hakika sisi ni wamtakiao wema?

Aya 8. *Waulizao,* yaani hao wanaotaka kujua ukweli wa Mtume Muhammad *s.a.w.* Aya hii pia inaonyesha ya kuwa kisa cha Nabii Yusuf hakikukusudiwa kiwe habari za maisha yake, bali kiwe dalili ya kuhakikisha ukweli wa Mtume Muhammad *s.a.w.* Kwa hakika katika maisha ya Nabii Yusuf mlikuwa na Ishara na bishara nyingi zilizokusudiwa baadaye zitimizwe katika maisha ya Mtume *s.a.w.*

13. Mpeleke kesho pamoja nasi atakula kwa furaha na kucheza, na bila shaka sisi tutamlinda.

اَرْسِلْهُ مَعَنَا غَدًا يَّرْتَعْ وَيَلْعَبْ وَاِنَّا لَهٗ لَحٰفِظُوْنَ ﴿١٣﴾

14. (Yakubu) akasema: Kwa hakika yananihuzunisha ninyi kwenda naye, na ninaogopa asije mbwa mwitu akamla hali ninyi mmeghafilika naye.

قَالَ اِنِّيْ لَيَحْزُنُنِيْٓ اَنْ تَذْهَبُوْا بِهٖ وَاَخَافُ اَنْ يَّاْكُلَهُ الذِّئْبُ وَاَنْتُمْ عَنْهُ غٰفِلُوْنَ ﴿١٤﴾

15. Wakasema: ikiwa mbwa mwitu atamla na hali sisi ni kundi lenye nguvu, basi hapo bila shaka tutakuwa wenye hasara.

قَالُوْا لَئِنْ اَكَلَهُ الذِّئْبُ وَنَحْنُ عُصْبَةٌ اِنَّآ اِذًا لَّخٰسِرُوْنَ ﴿١٥﴾

16. Basi walipomchukua na wakakubaliana kumtia katika shimo la kisima kirefu, mara Tukamfunulia: Bila shaka siku moja utawaambia jambo lao hili wakati hali hawatambui.

فَلَمَّا ذَهَبُوْا بِهٖ وَاَجْمَعُوْٓا اَنْ يَّجْعَلُوْهُ فِيْ غَيٰبَتِ الْجُبِّ ۚ وَاَوْحَيْنَآ اِلَيْهِ لَتُنَبِّئَنَّهُمْ بِاَمْرِهِمْ هٰذَا وَهُمْ لَا يَشْعُرُوْنَ ﴿١٦﴾

17. Na wakaja kwa baba yao usiku wakilia.

وَجَآءُوْٓ اَبَاهُمْ عِشَآءً يَّبْكُوْنَ ﴿١٧﴾ ؕ

18. Wakasema: Ewe baba yetu, hakika tulikwenda kushindana mbio na tukamwacha Yusuf penye vyombo vyetu, basi mbwa mwitu akamla, lakini huwezi kutuamini ingawa tunasema kweli.

قَالُوْا يٰٓاَبَانَآ اِنَّا ذَهَبْنَا نَسْتَبِقُ وَتَرَكْنَا يُوْسُفَ عِنْدَ مَتَاعِنَا فَاَكَلَهُ الذِّئْبُ ۚ وَمَآ اَنْتَ بِمُؤْمِنٍ لَّنَا وَلَوْ كُنَّا صٰدِقِيْنَ ﴿١٨﴾ ۚ

19. Na wakaleta kanzu yake yenye damu ya bandia. (Yakubu) akasema: bali nafsi zenu zimewafanyieni jambo hili kuwa zuri. Basi subira ni njema. Na Allah Ndiye Aombwaye msaada juu ya haya myasemayo.

وَجَآءُوْ عَلٰى قَمِيْصِهٖ بِدَمٍ كَذِبٍ ؕ قَالَ بَلْ سَوَّلَتْ لَكُمْ اَنْفُسُكُمْ اَمْرًا ؕ فَصَبْرٌ جَمِيْلٌ ؕ وَاللّٰهُ الْمُسْتَعَانُ عَلٰى مَا تَصِفُوْنَ ﴿١٩﴾

Aya 16. *Hali hawatambui*. Maneno haya yanagusia kuonyesha ya kwamba hali ya Yusuf ilikuwa ya unyonge sana hata nduguze hawakuweza kudhani kuwa atakuwa mtu mkubwa.

Aya 18. Padre Dale ametaka kuonyesha ya kwamba Qur'an haijapatana na Taurati katika masimulizi yake. Anasema, "Wala hatusomi ya kuwa walisema ya kwamba wameshindana kwa kwenda mbio. Walikuwa watu wazima kabisa" (uk. 614 wa tafsiri yake). Hakuna asemaye kuwa Qur'an na Taurati vimepatana katika mambo yote. Kama ingekuwa hivyo pasingekuwa na haja ya Qur'an tena.

وَجَآءَتْ سَيَّارَةٌ فَاَرْسَلُوْا وَارِدَهُمْ فَاَدْلٰى دَلْوَهٗ ؕ قَالَ يٰبُشْرٰى هٰذَا غُلٰمٌ ؕ وَاَسَرُّوْهُ بِضَاعَةً ؕ وَاللّٰهُ عَلِيْمٌۢ بِمَا يَعْمَلُوْنَ ۝٢٠

20. Na ukafika msafara, wakamtuma mteka maji wao, naye akatumbukiza ndoo yake. Akasema: Ee, habari njema! huyu hapa mvulana! Nao wakamficha kumfanya bidhaa. Na Allah Alijua sana waliyoyafanya.

وَشَرَوْهُ بِثَمَنٍۭ بَخْسٍ دَرَاهِمَ مَعْدُوْدَةٍ ۚ وَكَانُوْا فِيْهِ مِنَ الزّٰهِدِيْنَ ۝٢١ ع ١٤

21. Na (ndugu za Yusuf) wakamwuza kwa thamani hafifu kwa mapesa kidogo, na hawakuwa na haja nayo.

FUNGU 3

وَقَالَ الَّذِى اشْتَرٰىهُ مِنْ مِّصْرَ لِامْرَاَتِهٖٓ اَكْرِمِىْ مَثْوٰىهُ عَسٰٓى اَنْ يَّنْفَعَنَآ اَوْ نَتَّخِذَهٗ وَلَدًا ؕ وَكَذٰلِكَ مَكَّنَّا لِيُوْسُفَ فِى الْاَرْضِ ۖ وَلِنُعَلِّمَهٗ مِنْ تَاْوِيْلِ الْاَحَادِيْثِ ؕ وَاللّٰهُ غَالِبٌ عَلٰٓى اَمْرِهٖ وَلٰكِنَّ اَكْثَرَ النَّاسِ لَا يَعْلَمُوْنَ ۝٢٢

22. Na yule aliyemnunua katika Misri akamwambia mke wake: Mtengenezee makao ya heshima, huenda akatufaa au tukampanga kuwa mwana. Na hivyo ndivyo Tulivyomkalisha Yusuf katika nchi; ili tumfundishe hakika ya mambo. Na Allah ndiye Mshindi juu ya jambo Lake, lakini watu wengi hawajui.

وَلَمَّا بَلَغَ اَشُدَّهٗٓ اٰتَيْنٰهُ حُكْمًا وَّعِلْمًا ؕ وَكَذٰلِكَ نَجْزِى الْمُحْسِنِيْنَ ۝٢٣

23. Na (Yusuf) alipobalehe kikamilifu, Tukampa hukumu na elimu. Na hivi ndivyo Tunavyowalipa watendao mema.

وَرَاوَدَتْهُ الَّتِىْ هُوَ فِىْ بَيْتِهَا عَنْ نَّفْسِهٖ وَغَلَّقَتِ الْاَبْوَابَ وَقَالَتْ هَيْتَ لَكَ ؕ قَالَ مَعَاذَ اللّٰهِ اِنَّهٗ رَبِّىْٓ اَحْسَنَ مَثْوَاىَ ؕ اِنَّهٗ لَا يُفْلِحُ الظّٰلِمُوْنَ ۝٢٤

24. Na (mwanamke) ambaye nyumbani mwake (Yusuf) alikuwamo, akamtamani (Yusuf) kinyume cha radhi yake, na akafunga milango, na akasema: Njoo. (Yusuf) akasema: Najikinga kwa Allah. Bila shaka Yeye ndiye Mola wangu Ametengeneza kao langu vizuri. Hakika wadhalimu hawatastawi.

Dalili aliyotoa padre Dale ili kukadhibisha neno la Qur'an haina cho chote. Qur'an haisemi kwamba kweli walishindana mbio; bali wao walikwenda mwambia baba yao uwongo. Tena je, watu wazima hawashindani mbio? Hayo yaonyesha maelekeo ya mapadre ya kugeuza neno la Mungu kwa fikara zao zilizopindama.

وَلَقَدْ هَمَّتْ بِهٖ ۚ وَهَمَّ بِهَا لَوْلَاۤ اَنْ رَّاٰ بُرْهَانَ رَبِّهٖ ؕ كَذٰلِكَ لِنَصْرِفَ عَنْهُ السُّوْٓءَ وَالْفَحْشَآءَ ؕ اِنَّهٗ مِنْ عِبَادِنَا الْمُخْلَصِيْنَ ﴿۲۵﴾

25. Na hakika (mwanamke huyo) akamkazia nia (ya kumtaka), na (Yusuf) akamkazia nia (ya kumkimbia). Kama (Yusuf) asingaliona dalili ya Mola wake (asingaliweza kukaza nia ya namna hii). Hivi ndivyo ilivyotokea ili Tumwepushie kila jambo la aibu na uovu. Hakika yeye alikuwa katika watumishi Wetu waliohalisika.

وَاسْتَبَقَا الْبَابَ وَقَدَّتْ قَمِيْصَهٗ مِنْ دُبُرٍ وَّاَلْفَيَا سَيِّدَهَا لَدَا الْبَابِ ؕ قَالَتْ مَا جَزَآءُ مَنْ اَرَادَ بِاَهْلِكَ سُوْٓءًا اِلَّاۤ اَنْ يُّسْجَنَ اَوْ عَذَابٌ اَلِيْمٌ ﴿۲۶﴾

26. Na (wote wawili) wakakimbilia mlangoni, na mwanamke huyo akairarua kanzu yake kwa nyuma na wakamkuta mume wake mlangoni; mwanamke akasema: Hakuna malipo ya mwenye kutaka ubaya kwa mkeo isipokuwa kufungwa gerezani au kupewa adhabu iumizayo.

قَالَ هِيَ رَاوَدَتْنِيْ عَنْ نَّفْسِيْ ۚ وَشَهِدَ شَاهِدٌ مِّنْ اَهْلِهَا ۚ اِنْ كَانَ قَمِيْصُهٗ قُدَّ مِنْ قُبُلٍ فَصَدَقَتْ وَهُوَ مِنَ الْكٰذِبِيْنَ ﴿۲۷﴾

27. (Yusuf) akasema: Huyu mwanamke amenitaka bila mimi kutaka. Na shahidi aliyekuwa katika jamaa za mwanamke akatoa ushahidi (na akasema): Ikiwa kanzu yake imechanwa mbele, basi (mwanamke huyu) amesema kweli naye (Yusuf) yu katika waongo.

وَاِنْ كَانَ قَمِيْصُهٗ قُدَّ مِنْ دُبُرٍ فَكَذَبَتْ وَهُوَ مِنَ الصّٰدِقِيْنَ ﴿۲۸﴾

28. Na kama kanzu yake imechanwa nyuma, basi (mwanamke huyu) amesema uwongo naye (Yusuf) yu katika wakweli.

فَلَمَّا رَاٰ قَمِيْصَهٗ قُدَّ مِنْ دُبُرٍ قَالَ اِنَّهٗ مِنْ كَيْدِكُنَّ ؕ اِنَّ كَيْدَكُنَّ عَظِيْمٌ ﴿۲۹﴾

29. Basi (mumewe) alipoona kanzu yake imechanwa kwa nyuma, akasema: Hakika hii ni katika hila zenu wanawake. Bila shaka hila zenu ni kubwa.

يُوْسُفُ اَعْرِضْ عَنْ هٰذَا ۫ وَاسْتَغْفِرِيْ لِذَنْۢبِكِ ۖ اِنَّكِ كُنْتِ مِنَ الْخٰطِـِٕيْنَ ﴿۳۰﴾ ع ۱۳

30. Ewe Yusuf! achana nayo! na wewe mwanamke omba msamaha kwa dhambi yako. Hakika wewe ni mmoja wa wakosao.

Aya 25. Aya hii inatuambia ya kuwa mke wa bwana wa Yusuf alikusudia kumtendea Yusuf jambo ovu, lakini hakufanikiwa, maana Yusuf alifunga nia kabisa ya kujiepusha na ouvu wa yule mwanamke. Baadhi ya wafasiri wa zamani wamekosa kabisa katika kueleza Aya hii kwa vile walitaka kukifanya kiwe kisa kinachowapendeza. Nabii wa Allah ameepukana kabisa na madhambi ya kila namna.

FUNGU 4

وَقَالَ نِسْوَةٌ فِي الْمَدِيْنَةِ امْرَاَتُ الْعَزِيْزِ تُرَاوِدُ فَتٰىهَا عَنْ نَّفْسِهٖ ۚ قَدْ شَغَفَهَا حُبًّا ؕ اِنَّا لَنَرٰىهَا فِيْ ضَلٰلٍ مُّبِيْنٍ ﴿٣١﴾

31. Na wanawake wa mji ule wakasema: Mkewe waziri anamtamani mtumishi wake pasipo kutamaniwa naye. Hakika amemwathiri kwa mapenzi. Bila shaka sisi twamwona yumo katika upotevu dhahiri.

فَلَمَّا سَمِعَتْ بِمَكْرِهِنَّ اَرْسَلَتْ اِلَيْهِنَّ وَاَعْتَدَتْ لَهُنَّ مُتَّكَاً وَّاٰتَتْ كُلَّ وَاحِدَةٍ مِّنْهُنَّ سِكِّيْنًا وَّقَالَتِ اخْرُجْ عَلَيْهِنَّ ۚ فَلَمَّا رَاَيْنَهٗۤ اَكْبَرْنَهٗ وَقَطَّعْنَ اَيْدِيَهُنَّ وَقُلْنَ حَاشَ لِلّٰهِ مَا هٰذَا بَشَرًا ؕ اِنْ هٰذَاۤ اِلَّا مَلَكٌ كَرِيْمٌ ﴿٣٢﴾

32. Basi (mkewe waziri) aliposikia hila yao, akawaita na akawafanyia karamu na akampa kila mmoja wao kisu na akamwambia (Yusuf), jitokeze mbele yao. Basi walipomwona, wakamkuta ni aliyetukuka na wakaikata mikono yao (kwa kushangaa) na wakasema: Hasha lillahi; huyu si mwanadamu, huyu siye ila ni malaika mtukufu.

قَالَتْ فَذٰلِكُنَّ الَّذِيْ لُمْتُنَّنِيْ فِيْهِ ؕ وَلَقَدْ رَاوَدْتُّهٗ عَنْ نَّفْسِهٖ فَاسْتَعْصَمَ ؕ وَلَئِنْ لَّمْ يَفْعَلْ مَاۤ اٰمُرُهٗ لَيُسْجَنَنَّ وَلَيَكُوْنًا مِّنَ الصّٰغِرِيْنَ ﴿٣٣﴾

33. (Mkewe waziri) akasema: Huyu ndiye mliyenilaumia; na hakika nilimtamani kinyume cha nafsi yake, lakini akajilinda. Na kama hatafanya ninayomwamuru, bila shaka atafungwa gerezani na kwa yakini atakuwa miongoni mwa wadhalilifu.

قَالَ رَبِّ السِّجْنُ اَحَبُّ اِلَيَّ مِمَّا يَدْعُوْنَنِيْۤ اِلَيْهِ ۚ وَاِلَّا تَصْرِفْ عَنِّيْ كَيْدَهُنَّ اَصْبُ اِلَيْهِنَّ وَاَكُنْ مِّنَ الْجٰهِلِيْنَ ﴿٣٤﴾

34. (Yusuf) akasema: Ee Mola wangu! Naipenda zaidi gereza kuliko haya wanayoniitia; na kama Usiponiondoshea hila zao, nitawaelekea na nitakuwa miongoni mwa wajinga.

فَاسْتَجَابَ لَهٗ رَبُّهٗ فَصَرَفَ عَنْهُ كَيْدَهُنَّ ؕ اِنَّهٗ هُوَ السَّمِيْعُ الْعَلِيْمُ ﴿٣٥﴾

35. Basi Mola wake Akapokea maombi yake na Akamwondoshea hila zao. Bila shaka Yeye ndiye Asikiaye, Ajuaye.

Aya 32. *Malaika mtukufu.* Hapa ingawa nabii Yusuf ni mwanadamu, lakini kwa namna ya msemo, ameitwa "malaika" kwa maana ya mtu mwema, mtakatifu.

Maneno *Qat-twa'na aidiyahunna* (wakakata mikono yao) yaweza kueleweka kuwa yenye kutumika kwa maana ya neno kwa neno au kimethali kama vile Hadhrat Imam Raghib alivyotaja matumizi ya namna zote mbili alipokuwa akielezea matumizi ya neno hili ndani ya Qur'an Tukufu.

Hapa maana ya neno kwa neno ya *qat-twa'ana aidiyahunna* ingekuwa na maana ya kutengenisha mkono wa mtu na mwili wake kwa kutumia chombo kikali. Ni dhahiri kwamba hii

ثُمَّ بَدَا لَهُمْ مِّنْۢ بَعْدِ مَا رَاَوُا الْاٰيٰتِ لَيَسْجُنُنَّهٗ حَتّٰى حِيْنٍ ﴿٣٦﴾

36. Kisha ikawadhihirikia baada ya kuona alama, ya kuwa wamfunge kwa muda kidogo.

FUNGU 5

وَدَخَلَ مَعَهُ السِّجْنَ فَتَيٰنِ ؕ قَالَ اَحَدُهُمَآ اِنِّيْٓ اَرٰىنِيْٓ اَعْصِرُ خَمْرًا ۚ وَقَالَ الْاٰخَرُ اِنِّيْٓ اَرٰىنِيْٓ اَحْمِلُ فَوْقَ رَاْسِيْ خُبْزًا تَاْكُلُ الطَّيْرُ مِنْهُ ؕ نَبِّئْنَا بِتَاْوِيْلِهٖ ۚ اِنَّا نَرٰىكَ مِنَ الْمُحْسِنِيْنَ ﴿٣٧﴾

37. Na wakaingia pamoja naye gerezani vijana wawili. Mmoja wao akasema: Hakika nimejiona (katika ndoto) nakamua divai. Na mwingine akasema: Hakika nimejiona (katika ndoto) nabeba mikate juu ya kichwa changu ambayo ndege wanaila. Tuambie hakika yake; kwa yakini sisi tunakuona u miongoni mwa wafanyao hisani.

قَالَ لَا يَاْتِيْكُمَا طَعَامٌ تُرْزَقٰنِهٖٓ اِلَّا نَبَّاْتُكُمَا بِتَاْوِيْلِهٖ قَبْلَ اَنْ يَّاْتِيَكُمَا ؕ ذٰلِكُمَا مِمَّا عَلَّمَنِيْ رَبِّيْ ؕ اِنِّيْ تَرَكْتُ مِلَّةَ قَوْمٍ لَّا يُؤْمِنُوْنَ بِاللّٰهِ وَهُمْ بِالْاٰخِرَةِ هُمْ كٰفِرُوْنَ ﴿٣٨﴾

38. (Yusuf) akasema: Hakitawafikieni chakula mtakachopewa isipokuwa nitawaambieni hakika yake kabla hakijawafikieni. Hayo ni katika yale Aliyonifundisha Mola wangu. Hakika mimi nimeacha mila ya watu wasiomwamini Allah, na wao hawaiamini Akhera.

وَاتَّبَعْتُ مِلَّةَ اٰبَآءِيْٓ اِبْرٰهِيْمَ وَاِسْحٰقَ وَيَعْقُوْبَ ؕ مَا كَانَ لَنَآ اَنْ نُّشْرِكَ بِاللّٰهِ مِنْ شَيْءٍ ؕ ذٰلِكَ مِنْ فَضْلِ اللّٰهِ عَلَيْنَا وَعَلَى النَّاسِ وَلٰكِنَّ اَكْثَرَ النَّاسِ لَا يَشْكُرُوْنَ ﴿٣٩﴾

39. Na nimefuata mila ya baba zangu, Ibrahimu na Isihaka na Yakubu; hatuna haki ya kumshirikisha Allah na cho chote. Hiyo ni katika fadhili za Allah zilizo juu yetu na juu ya watu (wengine), lakini watu wengi hawashukuru.

siyo maana iliyokusudiwa na Qur'an Tukufu na haingii akilini katika maandishi haya. Katika kutafuta maana nyingine badala ya hii, baadhi ya wanazuoni wamejaribu kunasibisha maneno haya na kitendo hafifu cha ukataji chenye kuacha majeraha machache madogo madogo. Lakini matumizi ya lugha ya Kiarabu hayaungi mkono fikira hiyo kwa sababu ile nguvu na mshinikizo wa maana iliyomo katika mzizi wa neno (katika mizani ya *qat-twa'a*) hairuhusu uhafifu wa kitendo cha ukataji. Kwa hiyo chaguo pekee ni kati ya ile maana ya neno kwa neno na ile ya kimethali na tunaamini kwamba maneno haya yaliyomo katika maandishi husika yanaweza kueleweka vema kwa njia ya kimethali tu, ikiwa na maana kwamba walikubali kushindwa kwa kuona kwamba yeye ni mtu ambaye hawana uwezo wa kwenda kukutana naye, na mikono yao haiwezi kumfikia.

40. Enyi wafungwa wenzangu wawili, je, waungu wengi wanaofarakana ni bora au Allah Mmoja, Mwenye nguvu?

يٰصَاحِبَيِ السِّجْنِ ءَاَرْبَابٌ مُّتَفَرِّقُوْنَ خَيْرٌ اَمِ اللّٰهُ الْوَاحِدُ الْقَهَّارُ ۝٤٠

41. Hamwabudu badala yake ila majina matupu mliyoyapanga wenyewe na baba zenu; Allah Hakuteremsha dalili kwayo - hukumu siyo ila ni ya Allah. Ameamuru msimwabudu ye yote isipokuwa Yeye tu. Hiyo ndiyo dini isimamayo, lakini watu wengi hawajui.

مَا تَعْبُدُوْنَ مِنْ دُوْنِهٖۤ اِلَّاۤ اَسْمَآءً سَمَّيْتُمُوْهَاۤ اَنْتُمْ وَاٰبَآؤُكُمْ مَّاۤ اَنْزَلَ اللّٰهُ بِهَا مِنْ سُلْطٰنٍ ؕ اِنِ الْحُكْمُ اِلَّا لِلّٰهِ ؕ اَمَرَ اَلَّا تَعْبُدُوْۤا اِلَّاۤ اِيَّاهُ ؕ ذٰلِكَ الدِّيْنُ الْقَيِّمُ وَلٰكِنَّ اَكْثَرَ النَّاسِ لَا يَعْلَمُوْنَ ۝٤١

42. Enyi wafungwa wenzangu wawili! ama mmoja wenu atamnywesha bwana wake pombe; na ama mwingine, basi atauawa kwa kusulubiwa, na ndege watakula katika kichwa chake. Limekatwa jambo mlilokuwa mkiuliza.

يٰصَاحِبَيِ السِّجْنِ اَمَّاۤ اَحَدُكُمَا فَيَسْقِيْ رَبَّهٗ خَمْرًا ۚ وَاَمَّا الْاٰخَرُ فَيُصْلَبُ فَتَاْكُلُ الطَّيْرُ مِنْ رَّاْسِهٖ ؕ قُضِيَ الْاَمْرُ الَّذِيْ فِيْهِ تَسْتَفْتِيٰنِ ۝٤٢

43. Na (Yusufu) akamwambia yule aliyemdhania ya kwamba ataokoka katika wawili hawa: Unikumbuke mbele ya bwana wako. Lakini Shetani akamsahaulisha kumkumbuka kwa bwana wake, kwa hiyo akakaa gerezani miaka michache.

وَقَالَ لِلَّذِيْ ظَنَّ اَنَّهٗ نَاجٍ مِّنْهُمَا اذْكُرْنِيْ عِنْدَ رَبِّكَ ۖ فَاَنْسٰىهُ الشَّيْطٰنُ ذِكْرَ رَبِّهٖ فَلَبِثَ فِي السِّجْنِ بِضْعَ سِنِيْنَ ۝٤٣

FUNGU 6

44. Na mfalme akasema: Hakika mimi nimeona (ndotoni) ng'ombe saba wanono wanaliwa na ng'ombe saba walio dhaifu, na masuke saba mabichi na mengine yaliyokauka. Enyi wakubwa, niagulieni ndoto yangu ikiwa ninyi mnaweza kufasiri ndoto.

وَقَالَ الْمَلِكُ اِنِّيْۤ اَرٰى سَبْعَ بَقَرٰتٍ سِمَانٍ يَّاْكُلُهُنَّ سَبْعٌ عِجَافٌ وَّسَبْعَ سُنْۢبُلٰتٍ خُضْرٍ وَّاُخَرَ يٰبِسٰتٍ ؕ يٰۤاَيُّهَا الْمَلَاُ اَفْتُوْنِيْ فِيْ رُءْيَايَ اِنْ كُنْتُمْ لِلرُّءْيَا تَعْبُرُوْنَ ۝٤٤

Aya 41. Neno *Qayyim* kulingana na matumizi ya Qur'an Tukufu lina maana ya kuwa na nguvu, kuwa na mamlaka, kuwa sawasawa na kuwa na hali ya kudumu na kuwa na uwezo. Pia linaashiria uwezo wa kunyoosha na kusahihisha. Hivyo basi vijengea imani vya msingi na visivyobadilika vinavyopatikana katika dini zote vinarejewa katika Qura'n Tukufu kuwa ni *Diinul Qayyimah* (Tazama suratul Bayyinah 98:6).

قَالُوْٓا اَضْغَاثُ اَحْلَامٍ ۚ وَمَا نَحْنُ بِتَاْوِيْلِ الْاَحْلَامِ بِعٰلِمِيْنَ ﴿٤٤﴾

45. Wakasema: Ni ndoto zilizovurugika, wala sisi hatujui tafsiri ya ndoto hizi.

وَقَالَ الَّذِيْ نَجَا مِنْهُمَا وَادَّكَرَ بَعْدَ اُمَّةٍ اَنَا اُنَبِّئُكُمْ بِتَاْوِيْلِهٖ فَاَرْسِلُوْنِ ﴿٤٥﴾

46. Na akasema yule aliyeokoka katika wale (wafungwa) wawili na akakumbuka baada ya muda: Mimi nitawaambieni tafsiri yake, basi nitumeni.

يُوْسُفُ اَيُّهَا الصِّدِّيْقُ اَفْتِنَا فِيْ سَبْعِ بَقَرٰتٍ سِمَانٍ يَّاْكُلُهُنَّ سَبْعٌ عِجَافٌ وَّسَبْعِ سُنْۢبُلٰتٍ خُضْرٍ وَّاُخَرَ يٰبِسٰتٍ ۙ لَّعَلِّيْٓ اَرْجِعُ اِلَى النَّاسِ لَعَلَّهُمْ يَعْلَمُوْنَ ﴿٤٦﴾

47. Yusuf! ewe mkweli, tueleze hakika ya ng'ombe saba wanono kuliwa na ng'ombe saba dhaifu, na masuke saba mabichi na mengine yaliyokauka, ili nirejee kwa watu wapate kujua.

قَالَ تَزْرَعُوْنَ سَبْعَ سِنِيْنَ دَاَبًا ۚ فَمَا حَصَدْتُّمْ فَذَرُوْهُ فِيْ سُنْۢبُلِهٖٓ اِلَّا قَلِيْلًا مِّمَّا تَاْكُلُوْنَ ﴿٤٧﴾

48. Akasema: Mtalima miaka saba mfululizo kwa juhudi, na mtakavyovivuna, basi viacheni katika masuke yake, isipokuwa kidogo mnavyokula.

ثُمَّ يَاْتِيْ مِنْۢ بَعْدِ ذٰلِكَ سَبْعٌ شِدَادٌ يَّاْكُلْنَ مَا قَدَّمْتُمْ لَهُنَّ اِلَّا قَلِيْلًا مِّمَّا تُحْصِنُوْنَ ﴿٤٨﴾

49. Kisha itakuja baada ya hiyo miaka saba ya shida itakayokula vyote mlivyovitanguliza, isipokuwa kidogo mtakachohifadhi.

ثُمَّ يَاْتِيْ مِنْۢ بَعْدِ ذٰلِكَ عَامٌ فِيْهِ يُغَاثُ النَّاسُ وَفِيْهِ يَعْصِرُوْنَ ﴿٤٩﴾ ع

50. Kisha baada ya haya utakuja mwaka mmoja ambamo watu watasaidiwa na watapeana humo zawadi.

FUNGU 7

وَقَالَ الْمَلِكُ ائْتُوْنِيْ بِهٖ ۚ فَلَمَّا جَآءَهُ الرَّسُوْلُ قَالَ ارْجِعْ اِلٰى رَبِّكَ فَسْـَٔلْهُ مَا بَالُ النِّسْوَةِ الّٰتِيْ قَطَّعْنَ اَيْدِيَهُنَّ ۭ اِنَّ رَبِّيْ بِكَيْدِهِنَّ عَلِيْمٌ ﴿٥٠﴾

51. Na mfalme akasema: Mleteni kwangu. Basi mjumbe (wa mfalme) alipomfikia, (Yusuf) akasema: Rudi kwa bwana wako na ukamwulize imekuwaje shauri ya wanawake wale waliokata mikono yao; bila shaka Mola wangu Anazijua sana hila zao.

قَالَ مَا خَطْبُكُنَّ اِذْ رَاوَدْتُّنَّ يُوْسُفَ
عَنْ نَّفْسِهٖ ؕ قُلْنَ حَاشَ لِلّٰهِ مَا عَلِمْنَا
عَلَيْهِ مِنْ سُوْٓءٍ ؕ قَالَتِ امْرَاَتُ الْعَزِيْزِ
الْـٰٔنَ حَصْحَصَ الْحَقُّ ۫ اَنَا رَاوَدْتُّهٗ عَنْ
نَّفْسِهٖ وَاِنَّهٗ لَمِنَ الصّٰدِقِيْنَ ﴿٥١﴾

52. (Mfalme) akasema: Mlikuwa na kusudi gani mlipomtamani Yusuf kinyume na matamanio yake? Wakasema: Alijiepusha kwa ajili ya Allah tu, sisi hatukujua ubaya wo wote dhidi yake. Mkewe waziri akasema: Sasa haki imedhihirika, mimi ndiye nilimtamani kinyume cha nafsi yake, na bila shaka yeye yu miongoni mwa wakweli.

ذٰلِكَ لِيَعْلَمَ اَنِّيْ لَمْ اَخُنْهُ بِالْغَيْبِ وَاَنَّ
اللّٰهَ لَا يَهْدِيْ كَيْدَ الْخَآئِنِيْنَ ﴿٥٢﴾

53. (Yusuf akasema:) Hayo ni kwa sababu (Waziri) ajue ya kwamba mimi sikumfanyia hiyana nyuma yake na ya kwamba Allah Hazistawishi hila za mahaini.

JUZU 13

وَمَآ اُبَرِّئُ نَفْسِيْ ۚ اِنَّ النَّفْسَ ﴿٥٣﴾
لَاَمَّارَةٌۢ بِالسُّوْٓءِ اِلَّا مَا رَحِمَ رَبِّيْ ؕ
اِنَّ رَبِّيْ غَفُوْرٌ رَّحِيْمٌ ﴿٥٣﴾

54. Nami sijitakasi nafsi yangu; hakika nafsi ndiyo iamrishayo sana maovu, isipokuwa yule ambaye Mola wangu Amemrehemu. Hakika Mola wangu ni Msamehevu, Mrehemevu.

وَقَالَ الْمَلِكُ ائْتُوْنِيْ بِهٖٓ اَسْتَخْلِصْهُ
لِنَفْسِيْ ۚ فَلَمَّا كَلَّمَهٗ قَالَ اِنَّكَ الْيَوْمَ
لَدَيْنَا مَكِيْنٌ اَمِيْنٌ ﴿٥٥﴾

55. Na mfalme akasema: Mleteni kwangu, nimchague kwa ajili yangu mwenyewe. Basi alipozungumza naye, akasema: Hakika wewe leo kwetu u mwenye heshima, mwaminiwa.

Aya 54. *Sijitakasi nafsi yangu.* Maneno haya yalitamkwa na Nabii Yusuf. Aya hii inaonyesha jinsi Mitume wa Mungu na Wateule Wake walivyo na mioyo safi na tabia tukufu. Nabii Yusuf alitaka kesi ile ya kusingiziwa mambo ya aibu isikilizwe, siyo kwamba, asemavyo, ni haja yake kujionyesha kuwa yu mtakatifu. Anasema, kusudi lake ni kutaka kuonyesha ya kwamba Allah haachi fitina za watu wabaya zifanikiwe juu ya Manabii Wake, na ya kwamba hakuna mtu anayeweza kuwatia katika madhambi watu ambao Allah anawalinda.

Nabii Yusuf anakiri ya kwamba jinsi ya mwanadamu yenyewe tu bila rehema ya Allah haiwezi kujilinda na madhambi. Kwa kuepuka madhambi ni lazima mtu asaidiwe na rehema ya Mungu inayokuja kwa njia ya wahyi (ufunuo) na Sheria ya dini. Mpaka mtu aungane na Allah, kama vile Manabii na watu wema, ndipo anaweza kuepuka madhambi.

Annafsa la-ammaara, "Nafsi ndiyo iamrishayo sana." Soma maana ya maneno haya katika sura 75:3.

قَالَ اجْعَلْنِيْ عَلٰى خَزَآئِنِ الْاَرْضِ ۚ اِنِّيْ حَفِيْظٌ عَلِيْمٌ ﴿٥٦﴾

56. Akasema: Niweke juu ya hazina za nchi, hakika mimi ndiye nilindaye sana, nijuaye.

وَكَذٰلِكَ مَكَّنَّا لِيُوْسُفَ فِي الْاَرْضِ ۚ يَتَبَوَّاُ مِنْهَا حَيْثُ يَشَآءُ ؕ نُصِيْبُ بِرَحْمَتِنَا مَنْ نَّشَآءُ وَلَا نُضِيْعُ اَجْرَ الْمُحْسِنِيْنَ ﴿٥٧﴾

57. Na hivi ndivyo Tulivyompa Yusuf cheo katika nchi, akakaa humo po pote alipopenda. Tunamfikishia rehema Zetu Tumtakaye, wala Hatupotezi ujira wa wafanyao mema.

وَلَاَجْرُ الْاٰخِرَةِ خَيْرٌ لِّلَّذِيْنَ اٰمَنُوْا وَكَانُوْا يَتَّقُوْنَ ﴿٥٨﴾ ع

58. Na bila shaka ujira wa Akhera ni bora kwa wale walioamini na waliokuwa wakiogopa.

FUNGU 8

وَجَآءَ اِخْوَةُ يُوْسُفَ فَدَخَلُوْا عَلَيْهِ فَعَرَفَهُمْ وَهُمْ لَهٗ مُنْكِرُوْنَ ﴿٥٩﴾

59. Na wakaja ndugu za Yusuf na wakaingia kwake; basi akawajua, nao hawakumjua.

وَلَمَّا جَهَّزَهُمْ بِجَهَازِهِمْ قَالَ ائْتُوْنِيْ بِاَخٍ لَّكُمْ مِّنْ اَبِيْكُمْ ۚ اَلَا تَرَوْنَ اَنِّيْٓ اُوْفِي الْكَيْلَ وَاَنَا خَيْرُ الْمُنْزِلِيْنَ ﴿٦٠﴾

60. Na alipowaandali masurufu yao (kwa ajili ya safari) akasema: Nileteeni ndugu yenu aliyeko kwa baba yenu. Je hamwoni ya kwamba mimi ninatimiza kipimo nami ni mbora wa wakaribishao?

Aya 56. Aya hii inaonyesha ya kwamba hata Nabii wa Mungu anaweza kufanya kazi chini ya serikali isiyoshika dini yake, kama alivyofanya Nabii Yusuf.

Aya 59. Habari zinazoelezwa katika Aya hii zinahusu wakati ilipotokea njaa katika nchi, naye Yusuf alikuwa juu kabisa katika mamlaka.

Aya hii inaonyesha namna nyingine Mtume *s.a.w.* alivyofanana na Nabii Yusuf. Yusuf alitukuka kabisa hata nduguze wasiweze kumtambua kwa sababu wasingeweza kufikiri kuwa mtu tu waliyemtupa kisimani, kisha wakamwuza kama mtumwa angeweza kupata ukubwa wa kiasi kile. Namna hiyo hiyo watu wa Makka walistaajabia nguvu na heshima aliyopata Mtume *s.a.w.* Jambo hili linadhihirika katika namna aliyoshangaa Abu Sufyan, mkuu wa Makka. Heraclius (Hirakla), mfalme mkuu wa Kikristo aliyemiliki milki za Warumi za pande za mashariki, alipokea barua itokayo kwa Mtume *s.a.w.* ikimtarajia mfalme huyo aingine Uislamu. Heraclius alipoulizauliza habari za Mtume s.a.w. kwa Abu Sufyan ambaye wakati huo alikuwa Sham (Syria), akasema kumwambia Abu Sufyan, "Ikiwa hayo unayoniambia juu ya Mtume ni kweli, basi siku moja atatawala ardhi hii ninayoikanyaga." Maneno haya aliyosema mfalme mwenye nguvu kwa hiari yake yalimshangaza sana Abu Sufyan na akasema, "Kwa hakika jambo la Abu Kabsha limekuwa kubwa" (Bukhari, sura ya Jihadi). Ibni Abi Kabsha ni jina la dharau ambalo watu wa Makka walimpanga Mtume *s.a.w.*

Aya 60. Biblia inasema, Yusuf aliwaambia nduguze, "Mkaniletee ndugu yenu mdogo; ndipo nitakapojua kama ninyi si wapelelezi" (Mwanzo 42:34). Maneno haya yanaonyesha ya kwamba Yusuf aliwasema nduguze ni majasusi na kutishia kuwakamata. Lakini Qur'an inaonyesha

فَاِنْ لَّمْ تَاْتُوْنِیْ بِهٖ فَلَا كَیْلَ لَكُمْ عِنْدِیْ
وَلَا تَقْرَبُوْنِ ﴿۶۰﴾

61. Lakini kama hamtamleta kwangu, basi hamtakuwa na kipimo kwangu, wala msinikaribie.

قَالُوْا سَنُرَاوِدُ عَنْهُ اَبَاهُ وَاِنَّا لَفٰعِلُوْنَ ﴿۶۱﴾

62. Wakasema: Kwa yakini sisi tutamshawishi babaake kwa kumchukua, na kwa hakika sisi bila shaka tutafanya.

وَقَالَ لِفِتْیٰنِهِ اجْعَلُوْا بِضَاعَتَهُمْ فِیْ
رِحَالِهِمْ لَعَلَّهُمْ یَعْرِفُوْنَهَاۤ اِذَا انْقَلَبُوْۤا
اِلٰۤی اَهْلِهِمْ لَعَلَّهُمْ یَرْجِعُوْنَ ﴿۶۲﴾

63. Na (Yusuf) akawaambia watumishi wake: Tieni mali yao katika mizigo yao ili waione watakaporudi kwa watu wa nyumbani kwao, huenda watarejea.

فَلَمَّا رَجَعُوْۤا اِلٰۤی اَبِیْهِمْ قَالُوْا یٰۤاَبَانَا مُنِعَ
مِنَّا الْكَیْلُ فَاَرْسِلْ مَعَنَاۤ اَخَانَا نَكْتَلْ
وَاِنَّا لَهٗ لَحٰفِظُوْنَ ﴿۶۳﴾

64. Basi waliporejea kwa baba yao, wakasema: Ewe baba yetu, tumekataliwa kupimiwa (chakula), basi umtume ndugu yetu pamoja nasi ili tupate kupimiwa, na kwa yakini sisi tutamlinda.

قَالَ هَلْ اٰمَنُكُمْ عَلَیْهِ اِلَّا كَمَاۤ اَمِنْتُكُمْ
عَلٰۤی اَخِیْهِ مِنْ قَبْلُ ؕ فَاللّٰهُ خَیْرٌ حٰفِظًا ۪
وَّهُوَ اَرْحَمُ الرّٰحِمِیْنَ ﴿۶۴﴾

65. Akasema: Siwaaminini juu ya huyu isipokuwa kama nilivyowaaminini juu ya nduguye zamani. Basi Allah ni Mbora wa kulinda, naye ndiye Arehemuye kuliko warehemevu.

وَلَمَّا فَتَحُوْا مَتَاعَهُمْ وَجَدُوْا بِضَاعَتَهُمْ
رُدَّتْ اِلَیْهِمْ ؕ قَالُوْا یٰۤاَبَانَا مَا نَبْغِیْ ؕ

66. Na walipofungua vitu vyao, wakakuta bidhaa zao zimerejeshwa kwao. Wakasema: Ewe baba yetu, tunataka kingine nini? Hii mali yetu imerejeshwa

---

ya kwamba Yusuf aliwatendea nduguze kwa huruma. Inawezekana kwamba kwa kuwa Yusuf aliwadadisi mengi juu ya habari za nyumbani kwao na wazazi wao, nduguze wenyewe huenda walidhani ya kuwa pengine anawashuku kuwa majasusi. Kama si hivyo, haingewezekana Nabii wa Mungu kama Yusuf awaseme kuwa ni majasusi hali alijua kuwa ni nduguze. Yeye kusema hivyo ni sawa na kusema uwongo. Inaonekana kwamba Biblia inaeleza tu ilivyokuwa dhana ya nduguze Yusuf, na haikueleza hakika ya mambo kama hasa yalivyokuwa. Yusuf haielekei akilini kwamba angeweza kuwasema nduguze kuwa majasusi kwa kuwa hawakuja na mdogo wao Ben-yamini.

Aya 63. Ingawa Yusuf alijizuia sana asijibainishe kwa nduguze wakati alipowaona, lakini kuwapenda kwake kulimfanya awarudishie pesa zao. Si kama alifanya hiyana katika fedha ya serikali, kwani asingeshindwa kurejesha fedha ndogo kama ile kutoka mfukoni mwake.

Hapa pia Mtume *s.a.w.* amefanana sana na Yusuf kwa huruma juu ya nduguze, ingawa walimfanyia kila namna ya uovu kama alivyofanyiwa Yusuf. Angalia jinsi Mtume alivyokuwa na shauku nduguze wakubali haki, kama inavyoonekana katika maneno ya Aya hii, *Huenda utaangamiza nafsi yako kwa sababu hawawi waaminio* (sura 26:4).

هٰذِهٖ بِضَاعَتُنَا رُدَّتْ اِلَيْنَا ۚ وَنَمِيْرُ اَهْلَنَا وَنَحْفَظُ اَخَانَا وَنَزْدَادُ كَيْلَ بَعِيْرٍ ۭ ذٰلِكَ كَيْلٌ يَّسِيْرٌ ۝٦٥

kwetu! Na tutaleta chakula kwa ajili ya ahali zetu, na tutamlinda ndugu yetu, na tutapata zaidi kipimo cha ngamia mmoja: hicho ni kipimo chepesi.

قَالَ لَنْ اُرْسِلَهٗ مَعَكُمْ حَتّٰى تُؤْتُوْنِ مَوْثِقًا مِّنَ اللّٰهِ لَتَاْتُنَّنِيْ بِهٖٓ اِلَّآ اَنْ يُّحَاطَ بِكُمْ ۚ فَلَمَّآ اٰتَوْهُ مَوْثِقَهُمْ قَالَ اللّٰهُ عَلٰي مَا نَقُوْلُ وَكِيْلٌ ۝٦٦

67. Akasema: Sitamtuma pamoja nanyi kamwe mpaka mnipe ahadi kwa jina la Allah ya kwamba lazima mtamleta kwangu, isipokuwa mzungukwe (na hatari). Basi walipompa ahadi yao, akasema: Allah ndiye Msimamizi juu ya haya tusemayo.

وَقَالَ يٰبَنِيَّ لَا تَدْخُلُوْا مِنْۢ بَابٍ وَّاحِدٍ وَّادْخُلُوْا مِنْ اَبْوَابٍ مُّتَفَرِّقَةٍ ۭ وَمَآ اُغْنِيْ عَنْكُمْ مِّنَ اللّٰهِ مِنْ شَيْءٍ ۭ اِنِ الْحُكْمُ اِلَّا لِلّٰهِ ۭ عَلَيْهِ تَوَكَّلْتُ ۚ وَعَلَيْهِ فَلْيَتَوَكَّلِ الْمُتَوَكِّلُوْنَ ۝٦٧

68. Na akasema: Enyi wanangu msiingie katika mlango mmoja, bali mwingie katika milango mbalimbali; wala siwafaeni cho chote kwa Allah; hukumu haiko ila kwa Allah tu. Kwake nimetegemea, basi wategemeao na wategemee Kwake.

وَلَمَّا دَخَلُوْا مِنْ حَيْثُ اَمَرَهُمْ اَبُوْهُمْ ۭ مَا كَانَ يُغْنِيْ عَنْهُمْ مِّنَ اللّٰهِ مِنْ شَيْءٍ اِلَّا حَاجَةً فِيْ نَفْسِ يَعْقُوْبَ قَضٰىهَا ۭ وَاِنَّهٗ لَذُوْ عِلْمٍ لِّمَا عَلَّمْنٰهُ وَلٰكِنَّ اَكْثَرَ النَّاسِ لَا يَعْلَمُوْنَ ۝٦٨ ع

69. Na walipoingia jinsi alivyowaamuru baba yao, haikuwafaa kitu kwa Allah, isipokuwa haja iliyokuwa katika nafsi ya Yakubu aliitimiza. Na bila shaka yeye alikuwa mwenye elimu kwa sababu Tulimfundisha, lakini watu wengi hawajui.

FUNGU 9

وَلَمَّا دَخَلُوْا عَلٰي يُوْسُفَ اٰوٰٓى اِلَيْهِ اَخَاهُ قَالَ اِنِّيْٓ اَنَا اَخُوْكَ فَلَا تَبْتَىِٕسْ بِمَا كَانُوْا يَعْمَلُوْنَ ۝٦٩

70. Na walipoingia kwa Yusuf, akamkalisha ndugu yake karibu yake, akasema: Hakika mimi ni ndugu yako, basi usihuzunike kwa sababu ya yale waliyokuwa wakiyafanya.

فَلَمَّا جَهَّزَهُمْ بِجَهَازِهِمْ جَعَلَ

71. Na alipokwisha wapatia chakula chao, akaweka kikombe cha kunywea

Aya 68. *Mwingie katika milango mbalimbali.* Ndugu za Yusuf walikuwa wamemwambia baba yao ya kuwa huko Misri walishukiwa kwamba wao ni wapelelezi. Basi, safari hii baba yao akawaambia watakapofika waingie katika milango mbalimbali ili shuku ya watu isizidi.

Aya 71. Neno *ja'ala* (akaweka) linaweza kuwa na maana mbili: ama Yusuf aliamuru

السِّقَايَةَ فِيْ رَحْلِ اَخِيْهِ ثُمَّ اَذَّنَ مُؤَذِّنٌ
اَيَّتُهَا الْعِيْرُ اِنَّكُمْ لَسٰرِقُوْنَ ﴿٧٠﴾

maji (bila kujua) katika mzigo wa nduguye. Kisha mnadi akanadi: Enyi wasafiri, hakika ninyi ni wezi.

قَالُوْا وَاَقْبَلُوْا عَلَيْهِمْ مَّاذَا تَفْقِدُوْنَ ﴿٧١﴾

72. Wakasema wakiwaelekea: Mmepoteza nini?

قَالُوْا نَفْقِدُ صُوَاعَ الْمَلِكِ وَلِمَنْ جَآءَ بِهٖ
حِمْلُ بَعِيْرٍ وَّاَنَا بِهٖ زَعِيْمٌ ﴿٧٢﴾

73. Wakasema: Tumepoteza pishi ya mfalme, na atakayeileta atapewa mzigo wa ngamia, nami ni mdhamini wake.

قَالُوْا تَاللّٰهِ لَقَدْ عَلِمْتُمْ مَّا جِئْنَا لِنُفْسِدَ
فِي الْاَرْضِ وَمَا كُنَّا سٰرِقِيْنَ ﴿٧٣﴾

74. Wakasema: Wallahi mmekwisha jua ya kwamba sisi hatukuja kufanya uharibifu katika nchi, wala sisi si wezi.

قَالُوْا فَمَا جَزَآؤُهٗٓ اِنْ كُنْتُمْ كٰذِبِيْنَ ﴿٧٤﴾

75. Wakasema: Basi malipo yake yatakuwa nini kama ninyi mwasema uwongo?

قَالُوْا جَزَآؤُهٗ مَنْ وُّجِدَ فِيْ رَحْلِهٖ فَهُوَ
جَزَآؤُهٗ ؕ كَذٰلِكَ نَجْزِي الظّٰلِمِيْنَ ﴿٧٥﴾

76. Wakasema: Malipo yake ni ambaye itaonekana katika mzigo wake basi yeye ndiye malipo yake! Hivi ndivyo tuwalipavyo wadhalimu.

kikombe kitiwe katika mzigo wa nduguye hali akijua ili aweze kukitumia kwa kunywea maji njiani; au kilitiwa mle mzigoni kwa bahati mbaya: yaani baada ya Yusuf kunywa maji alipokuwa anazungumza na nduguye, kikombe kikapata kuwekwa pamoja na vitu vya Ben-yamini, hali Yusuf hana habari kama kiko pale.

Aya 73. Aya hii na zinazofuata zimebishaniwa sana na wafasiri wa Qur'an. Wanalaumu ya kuwa Nabii Yusuf aliweka makusudi kikombe katika mzigo wa nduguye, kisha akamkamatisha wizi apate kubakia naye. Kufikiri tafsiri ya namna hii ni ovyo kabisa. Jambo kama hili halimpasi Nabii wa Mungu, kumsingizia mtu na kusema uwongo na kumfedhehesha bure mbele za watu. Habari zenyewe zilikuwa hivi:

Kilichopotea siku ile ni pishi ya mfalme *(suwaa 'al-malik)*; na kitu Yusuf alichotia katika mfuko wa nduguye ni kikombe cha kunywea maji *(siqaayat)* ili kiweze kumsaidia njiani. Lakini kwa bahati mbaya, pishi aliyokuwa nayo mkononi ilibakia katika mzigo ule wakati akitia kikombe, hali kabisa hana habari, katika makiwa ya kuagana na nduguye mpenzi. Walipokwisha ondoka, kuzindukana, pishi haipo, na hajui nani ameichukua. Ikalazimu watazamwe wasafiri. Kwa heshima ya Yusuf, mzigo wa nduguye haukutazamwa ila mwisho, na kumbe pishi ikapatikana humo. Mara Yusuf akajua kuwa Mungu amemtengenezea hila hii ili aweze kubakia na mdogo wake.

Aya 76. Allah alitengeneza shauri hili kwa namna ambayo hata wale ndugu za Yusuf katika wasiwasi wao wakasema, mtu atakayekutwa nayo pishi ile, basi huyo azuiwe. Kwa ajili hii Yusuf akaweza kumzuia nduguye. Lau kama wangesema ya kuwa mtu atakayehakikishwa kuwa ndiye mwizi, huyo azuiwe, Nabii Yusuf asingeweza kumzuia nduguye; maana alijua si mwizi na hakuiba.

77. Basi akaanza na mizigo yao kabla ya mzigo wa nduguye; kisha akaitoa katika mzigo wa nduguye. Hivi ndivyo Tulivyomfanyia mpango Yusuf. Hakuweza kumzuia nduguye kwa kanuni ya mfalme, isipokuwa alivyotaka Allah. Tunamwinua vyeo yule Tumtakaye; na juu ya kila mwenye elimu yuko Ajuaye zaidi.

فَبَدَاَ بِاَوْعِيَتِهِمْ قَبْلَ وِعَآءِ اَخِيْهِ ثُمَّ اسْتَخْرَجَهَا مِنْ وِّعَآءِ اَخِيْهِ ؕ كَذٰلِكَ كِدْنَا لِيُوْسُفَ ؕ مَا كَانَ لِيَاْخُذَ اَخَاهُ فِيْ دِيْنِ الْمَلِكِ اِلَّاۤ اَنْ يَّشَآءَ اللّٰهُ ؕ نَرْفَعُ دَرَجٰتٍ مَّنْ نَّشَآءُ ؕ وَفَوْقَ كُلِّ ذِيْ عِلْمٍ عَلِيْمٌ ﴿۷۷﴾

78. Wakasema: Kama amekwiba, basi ndugu yake pia alikwiba zamani. Lakini Yusuf akayasiri moyoni mwake wala hakuwadhihirishia. Akasema: Ninyi mna hali mbaya; na Allah Anajua mnayoyasema.

قَالُوْۤا اِنْ يَّسْرِقْ فَقَدْ سَرَقَ اَخٌ لَّهٗ مِنْ قَبْلُ ۚ فَاَسَرَّهَا يُوْسُفُ فِيْ نَفْسِهٖ وَلَمْ يُبْدِهَا لَهُمْ ۚ قَالَ اَنْتُمْ شَرٌّ مَّكَانًا ۚ وَاللّٰهُ اَعْلَمُ بِمَا تَصِفُوْنَ ﴿۷۸﴾

79. Wakasema: Ewe Mheshimiwa, hakika anaye baba mzee sana, kwa hiyo mshike mmoja wetu badala yake; bila shaka sisi tunakuona u miongoni mwa wafanyao ihsani.

قَالُوْا يٰۤاَيُّهَا الْعَزِيْزُ اِنَّ لَهٗۤ اَبًا شَيْخًا كَبِيْرًا فَخُذْ اَحَدَنَا مَكَانَهٗ ۚ اِنَّا نَرٰىكَ مِنَ الْمُحْسِنِيْنَ ﴿۷۹﴾

80. Akasema: Allah Apishe mbali! Hatuwezi kumkamata isipokuwa yule tuliyekuta mali yetu iko kwake; tusije kuwa wadhalimu.

قَالَ مَعَاذَ اللّٰهِ اَنْ نَّاْخُذَ اِلَّا مَنْ وَّجَدْنَا مَتَاعَنَا عِنْدَهٗۤ ۙ اِنَّاۤ اِذًا لَّظٰلِمُوْنَ ﴿۸۰﴾ ع

Aya 77. *Hivi ndivyo Tulivyomfanyia hila Yusuf.* Maneno haya yanaonyesha wazi bila taabu ya kuwa habari yote ilipangwa na Allah Mwenyewe, si Nabii Yusuf.

Hakuweza kumzuia nduguye kwa kanuni ya mfalme. Maneno haya yanaonyesha ya kuwa hata Nabii aliye chini ya serikali ya watu baki lazima afuate amri zake na kuzisaidia. Nabii Yusuf alipenda abakie na nduguye, lakini sheria ya nchi haikumruhusu. Bali kudura ya Mungu ikamtoshelezea haja yake. Waislamu wanaodhani kwamba serikali isiyo ya Kiislamu si haki yao kuitiii kwa uaminifu na kuisaidia wanakosea vibaya sana, wala katika dini ya Kiisalmu hakuna fundisho la namna hiyo.

Aya 78. Nduguze Yusuf kwanza walitaka kumwua, na sasa bila kuona haya wanasema, ati yeye Yusuf naye alikuwa mwizi kama huyu nduguye aliyekamatwa. Jambo la kustaajabisha ni kuwa baadhi ya wafasiri, badala ya kupuuza maneno haya ya uwongo, wakaanza kutafutatafuta ni lini Yusuf alipata kwiba; na tashwishi zao zimewafanya wazuke na maneno ya kuwa ati Yusuf aliwahi kwiba vitu vichache nyumbani kwa shangazi yake, na kadha wa kadha!

Aya 80. Aya hii inabatilisha kabisa fundisho la Kikristo la kafara, lisemalo kuwa watu wengine wamefanya dhambi na Yesu akauawa ili kuwa fidia ya dhambi zao na kuwakomboa. Nabii Yusuf anasema, hangefanya haki kumzuia mtu asiye na kosa mahali pa mtu aliyekosa,

FUNGU 10

فَلَمَّا اسْتَيْـَٔسُوْا مِنْهُ خَلَصُوْا نَجِيًّا ؕ قَالَ
كَبِيْرُهُمْ اَلَمْ تَعْلَمُوْۤا اَنَّ اَبَاكُمْ قَدْ اَخَذَ
عَلَيْكُمْ مَّوْثِقًا مِّنَ اللّٰهِ وَمِنْ قَبْلُ مَا
فَرَّطْتُّمْ فِيْ يُوْسُفَ ۚ فَلَنْ اَبْرَحَ
الْاَرْضَ حَتّٰى يَاْذَنَ لِيْۤ اَبِيْۤ اَوْ يَحْكُمَ اللّٰهُ
لِيْ ۚ وَهُوَ خَيْرُ الْحٰكِمِيْنَ ﴿۸۱﴾

81. Basi walipomkatia tamaa, wakaenda kando kunong'ona. Mkubwa wao akasema: Je, hamjui ya kwamba baba yenu ameshika juu yenu ahadi kwa jina la Allah, na zamani pia mlikosa katika agano juu ya Yusuf? Basi sitaitoka nchi hii mpaka baba yangu aniruhusu au Allah Anihukumu. Naye ni Mbora wa mahakimu.

اِرْجِعُوْۤا اِلٰۤى اَبِيْكُمْ فَقُوْلُوْا يٰۤاَبَانَاۤ اِنَّ
ابْنَكَ سَرَقَ ۚ وَمَا شَهِدْنَاۤ اِلَّا بِمَا عَلِمْنَا
وَمَا كُنَّا لِلْغَيْبِ حٰفِظِيْنَ ﴿۸۲﴾

82. Rudini kwa baba yenu, na semeni: Ee baba yetu, hakika mwanao ameiba, na sisi hatukushuhudia isipokuwa yale tuliyoyajua na hatukuwa walindao yaliyokuwa katika siri.

وَسْـَٔلِ الْقَرْيَةَ الَّتِيْ كُنَّا فِيْهَا وَالْعِيْرَ الَّتِيْۤ
اَقْبَلْنَا فِيْهَا ؕ وَاِنَّا لَصٰدِقُوْنَ ﴿۸۳﴾

83. Na waulize watu wa mji tuliokuwa na msafara tuliofika nao; na hakika sisi tunasema kweli.

---

ingawa nduguze Yusuf walijitoa kwa hiari zao wafungwe na mdogo wao akomboke. Biblia pia inashirikiana na Qur'an katika kubatilisha hii kafara anayosingiziwa nayo Yesu. Inasema, ndugu za Ben-yamini walipotaka wazuiwe wao na Ben-yamini aachiwe, Yusuf alijibu, "Hasha! nisifanye hivi; mtu ambaye kikombe kilionekana mkononi mwake, ndiye atakayekuwa mtumwa wangu. Nanyi enendeni zenu kwa amani kwa baba yenu." (Mwanzo 42:17). Mbele ya makanusho kama haya ya Biblia kwamba asiye na kosa hakubaliwi kujitoa aadhibiwe mahali pa aliye na kosa, ingewezekanaje mateso ya Yesu kuwa fidia ya dhambi za wafuasi wake?

Aya 81. *Kabiiruhum,* "Mkubwa wao." Neno *kabiir* lina maana ya: kiongozi; mwenye mwili mkubwa; mkubwa au aliyekwisha kua; mwenye elimu au ajuaye zaidi; mwalimu au mkufunzi; mkuu wa watu; mzee au mwenye umri mwingi (Mufradat).

Waandishi wabishi wa Kikristo wanasema ya kuwa Qur'an imekosa katika kusema ya kwamba ni "mkubwa wao" aliyewaambia nduguze maneno yaliyomo katika Aya hii. Wanasema ya kuwa ni Yuda, wa nne kuzaliwa, aliyewaambia ndugu zake hayo, wala si Ruben aliyekuwa mkubwa wa wao wote. Ni jambo la kushangaza ya kwamba hawa mabwana wanaojipa uhakimu juu ya Qur'an, kila wanapokuta habari za Biblia ni tofauti na Qur'an, basi, Qur'an imekosa na Biblia ndiyo sawa! Hali imekwisha hakikishwa hata na waandishi wa Kikristo wenzao kuwa Biblia yao haiwezi kamwe, kutegemewa kuwa ni taarifa sahihi ya historia.

Lakini hata kama, kwa mathali ya maneno, tuseme kuwa maelezo ya Biblia ni sahihi, maelezo ya Qur'an hayawezi kutolewa makosa. Neno ambalo Qur'an imelitumia juu ya ndugu yao aliyekataa kwenda ni *kabiir* yaani "mkubwa"; haikutumia neno *akbar* ambalo maana yake ni "mkubwa wa wote." Kwa kuwa Yuda alikuwa ni ndugu wa nne katika watoto kumi na mbili, ni wazi alikuwa mmoja katika ndugu wakubwa wa Yusuf.

قَالَ بَلْ سَوَّلَتْ لَكُمْ اَنْفُسُكُمْ اَمْرًا ؕ
فَصَبْرٌ جَمِيْلٌ ؕ عَسَى اللّٰهُ اَنْ يَّاْتِيَنِيْ
بِهِمْ جَمِيْعًا ؕ اِنَّهٗ هُوَ الْعَلِيْمُ الْحَكِيْمُ ﴿٨٣﴾

84. (Yakubu) akasema:(Hapana) bali nafsi zenu zimelifanya jambo kubwa sana lionekane kwenu kuwa dogo na la kawaida. Basi subira ni njema, huenda Allah Akaniletea wote pamoja. Hakika Yeye ni Mjuzi, Mwenye Hekima.

وَتَوَلّٰى عَنْهُمْ وَقَالَ يٰۤاَسَفٰى عَلٰى
يُوْسُفَ وَابْيَضَّتْ عَيْنٰهُ مِنَ الْحُزْنِ
فَهُوَ كَظِيْمٌ ﴿٨٤﴾

85. Na akajitenga nao na akasema: Oo majonzi juu ya Yusuf! Na macho yake yakajawa na machozi kwa sababu ya huzuni, naye akawa anaizuia huzuni yake.

قَالُوْا تَاللّٰهِ تَفْتَؤُا تَذْكُرُ يُوْسُفَ حَتّٰى
تَكُوْنَ حَرَضًا اَوْ تَكُوْنَ مِنَ الْهٰلِكِيْنَ ﴿٨٥﴾

86. Wakasema: Wallahi, hutaacha kuzungumza juu ya Yusuf mpaka uwe mgonjwa au uwe miongoni mwa waangamiao.

قَالَ اِنَّمَاۤ اَشْكُوْا بَثِّيْ وَحُزْنِيْۤ اِلَى اللّٰهِ
وَاَعْلَمُ مِنَ اللّٰهِ مَا لَا تَعْلَمُوْنَ ﴿٨٦﴾

87. Akasema: Hakika mimi nashtakia sikitiko langu na huzuni yangu kwa Allah; na ninayajua toka kwa Allah msiyoyajua.

يٰبَنِيَّ اذْهَبُوْا فَتَحَسَّسُوْا مِنْ يُّوْسُفَ
وَاَخِيْهِ وَلَا تَايْـَٔسُوْا مِنْ رَّوْحِ اللّٰهِ ؕ
اِنَّهٗ لَا يَايْـَٔسُ مِنْ رَّوْحِ اللّٰهِ اِلَّا
الْقَوْمُ الْكٰفِرُوْنَ ﴿٨٧﴾

88. Enyi wanangu, nendeni na mkamtafute Yusuf na nduguye, wala msikate tamaa katika rehema ya Allah; hakika hawakati tamaa ya rehema ya Allah isipokuwa watu makafiri.

فَلَمَّا دَخَلُوْا عَلَيْهِ قَالُوْا يٰۤاَيُّهَا الْعَزِيْزُ
مَسَّنَا وَاَهْلَنَا الضُّرُّ وَجِئْنَا بِبِضَاعَةٍ

89. Basi walipoingia kwake wakasema: Ewe Mheshimiwa, shida imetupata sisi na ahali zetu, na tumeleta mali kidogo,

Tena neno *kabiiruhum* maana yake ni "kiongozi wao" au "mkubwa" kwa cheo na heshima. Na inaoenekana katika Biblia ya kuwa tabia mbaya za ndugu wakubwa watatu wa Yuda zilifanya Yuda awe mbele yao (Mwanzo 49:3-8). Yuda alikuwa mkubwa kuliko Ruben katika macho ya Nabii Yakubu, baba yao, hata inaonekana ya kwamba Ruben alipotoa watoto wake wawili wawe dhamana kwa ajili ya kumchukua Ben-yamini aende naye Misri, Yakubu alikataa (Mwanzo 42:37, 38). Lakini Yuda aliposema, "Mimi nitakuwa mdhamini wake," Yakubu akakubali (Mwanzo 43:9-10). Qur'an iliposema "mkubwa wao" mradi ni mkubwa wa heshima.

Aya 85. *Macho yake yakawa meupe kwa huzuni.* Wanaotafsiri maneno haya kuwa Nabii Yakubu alipofuka macho, wamekosa kabisa. Macho kuwa meupe kwa huzuni siyo maana yake kupofuka. Allah anasema, Nabii Yakubu *alikuwa akizuia (huzuni).* Sasa haiwezekani mwenye kuvumilia huzuni aanze kulia kwa huzuni hata apofuke. Zaidi ya hayo, haimstahili Nabii wa Mungu kulilia kitu cha kidunia japo kikubwa namna gani, kucha kutwa, hata apofuke macho.

Aya 88. Aya hii inaonyesha ya kuwa Allah alimjulisha Nabii Yakubu ya kuwa Yusuf yungali hai na yuko Misri; maana anawatuma wanawe waende Misri kumtafuta.

مُّزْجٰىةٍ فَاَوْفِ لَنَا الْكَيْلَ وَتَصَدَّقْ
عَلَيْنَا ؕ اِنَّ اللّٰهَ يَجْزِى الْمُتَصَدِّقِيْنَ ﴿٨٨﴾

kwa hiyo tupimie kipimo kamili na utuzidishie (kama sadaka). Hakika Allah huwalipa watoao sadaka.

قَالَ هَلْ عَلِمْتُمْ مَّا فَعَلْتُمْ بِيُوْسُفَ
وَاَخِيْهِ اِذْ اَنْتُمْ جٰهِلُوْنَ ﴿٨٩﴾

90. Akasema: Je, mnajua mliyomfanyia Yusuf na nduguye mlipokuwa ujingani?

قَالُوْٓا ءَاِنَّكَ لَاَنْتَ يُوْسُفُ ؕ قَالَ اَنَا
يُوْسُفُ وَهٰذَآ اَخِىْ ۖ قَدْ مَنَّ اللّٰهُ عَلَيْنَا ؕ
اِنَّهٗ مَنْ يَّتَّقِ وَيَصْبِرْ فَاِنَّ اللّٰهَ لَا يُضِيْعُ
اَجْرَ الْمُحْسِنِيْنَ ﴿٩٠﴾

91. Wakasema: Je, hakika wewe ndiwe Yusuf? Akasema: Mimi ndiye Yusuf na huyu ni ndugu yangu. Bila shaka Allah Ametufanyia hisani, hakika anayemcha Mungu na kusubiri, basi hakika Allah Hapotezi ujira wa wafanyao mema.

قَالُوْا تَاللّٰهِ لَقَدْ اٰثَرَكَ اللّٰهُ عَلَيْنَا وَاِنْ كُنَّا
لَخٰطِـِٕيْنَ ﴿٩١﴾

92. Wakasema: Wallahi bila shaka Allah Amekuchagua juu yetu, na hakika sisi tulikuwa wenye hatia.

قَالَ لَا تَثْرِيْبَ عَلَيْكُمُ الْيَوْمَ ؕ يَغْفِرُ اللّٰهُ
لَكُمْ ۖ وَهُوَ اَرْحَمُ الرّٰحِمِيْنَ ﴿٩٢﴾

93. Akasema: Hakuna lawama juu yenu leo; Allah Awasameheni, naye ni Mrehemevu zaidi kuliko wanaorehemu.

اِذْهَبُوْا بِقَمِيْصِىْ هٰذَا فَاَلْقُوْهُ عَلٰى وَجْهِ
اَبِىْ يَاْتِ بَصِيْرًا ۚ وَاْتُوْنِىْ بِاَهْلِكُمْ
اَجْمَعِيْنَ ﴿٩٣﴾ ع

94. Nendeni na kanzu yangu hii na muiweke mbele ya uso wa baba yangu; yeye atatambua. Na nijieni pamoja na ahali zenu nyote.

Aya 91. Namna Nabii Yusuf alivyowatajia nduguze tabia yao ya zamani, pamoja na maneno waliyokuwa wakisikia kwa baba yao kuwa Yusuf yu hai, ikawafanya nduguze hapa wamwulize kama yeye ndiye Yusuf. Basi Nabii Yusuf hakutaka tena kuwakawiza, akawajibu kuwa ndiye yeye. Na kwa upole akawaambia ya kuwa mtu hawezi kufanikiwa isipokuwa kwa utawa na subira, kwa kufanya kazi kwa bidii na kwa kumtegemea Mungu ambaye ni Rafiki wa watu wema na anawalinda.

Aya 93. Aya hii inaonyesha utukufu wa tabia ya Nabii Yusuf. Hakungoja nduguze wamtake radhi, bali mara moja akawatoa shaka na hofu ya kuwa hatolipiza kisasi.

Kama vile Nabii Yusuf, Mtume *s.a.w.* katika kuhama kwake alipata nguvu na mamlaka, na akairudia Makka pamoja na masahaba elfu kumi. Makka ilishindwa na akawauliza wenyeji wake, wanatazamia awatendee nini. Wakajibu, "Namna Yusuf alivyowatendea nduguze." Basi akawaambia. "Hakuna lawama juu yenu leo." Wema huu wa Mtume *s.a.w.* kwa maadui zake waliofanya kila namna ya juhudi wapate kumwua, hauna mfano katika historia ya wanadamu.

Aya 94. *Atatambua,* yaani zamani alijua kwa ufunuo tu ya kuwa Yusuf yu hai, na ujuzi wake ulikuwa ni wa imani tu. Lakini kwa kuona kanzu yake imani ile itapinduka kuwa ujuzi hasa.

FUNGU 11

وَلَمَّا فَصَلَتِ الْعِيْرُ قَالَ اَبُوْهُمْ اِنِّيْ
لَاَجِدُ رِيْحَ يُوْسُفَ لَوْلَآ اَنْ تُفَنِّدُوْنِ ﴿٩٤﴾

95. Na ulipoondoka msafara, baba yao akasema: Hakika napata harufu ya Yusuf isije mkanidhani ni zuzu.

قَالُوْا تَاللّٰهِ اِنَّكَ لَفِيْ ضَلٰلِكَ الْقَدِيْمِ ﴿٩٥﴾

96. Wakasema: Wallahi hakika ungali katika upotevu wako wa zamani

فَلَمَّآ اَنْ جَآءَ الْبَشِيْرُ اَلْقٰىهُ عَلٰى وَجْهِهٖ
فَارْتَدَّ بَصِيْرًا ۚ قَالَ اَلَمْ اَقُلْ لَّكُمْ ۚ اِنِّيْٓ
اَعْلَمُ مِنَ اللّٰهِ مَا لَا تَعْلَمُوْنَ ﴿٩٦﴾

97. Basi alipofika mtoaji wa habari njema, akaiweka (kanzu ya Yusuf) mbele ya uso wake ndipo akawa mwenye kutambua. Akasema: Je, sikuwaambieni, Hakika mimi nayajua toka kwa Allah msiyoyajua?

قَالُوْا يٰٓاَبَانَا اسْتَغْفِرْ لَنَا ذُنُوْبَنَآ اِنَّا
كُنَّا خٰطِـِٕيْنَ ﴿٩٧﴾

98. Wakasema: Ewe baba yetu, tuombee msamaha kwa dhambi zetu; bila shaka sisi tulikuwa wenye hatia.

قَالَ سَوْفَ اَسْتَغْفِرُ لَكُمْ رَبِّيْ ۭ اِنَّهٗ
هُوَ الْغَفُوْرُ الرَّحِيْمُ ﴿٩٨﴾

99. Akasema: Bila shaka nitawaombeeni msamaha kwa Mola wangu; hakika Yeye ndiye Msamehevu, Mrehemevu.

فَلَمَّا دَخَلُوْا عَلٰى يُوْسُفَ اٰوٰٓى اِلَيْهِ
اَبَوَيْهِ وَقَالَ ادْخُلُوْا مِصْرَ اِنْ شَاۗءَ اللّٰهُ
اٰمِنِيْنَ ﴿٩٩﴾

100. Na walipoingia kwa Yusuf, akawaweka kwake wazazi wake na akasema: Ingieni Misri, inshallah, kwa amani.

وَرَفَعَ اَبَوَيْهِ عَلَى الْعَرْشِ وَخَرُّوْا لَهٗ
سُجَّدًا ۚ وَقَالَ يٰٓاَبَتِ هٰذَا تَاْوِيْلُ رُءْيَايَ
مِنْ قَبْلُ ۡ قَدْ جَعَلَهَا رَبِّيْ حَقًّا ۭ وَقَدْ

101. Na akawanyanyua wazazi wake na kuwaweka kitini, na wote wakaporomoka kumsujudia (Allah). Na akasema: Ewe babaangu, hii ndiyo taabiri ya ndoto yangu ya zamani.

Aya 100. Mama aliyemzaa Yusuf alikuwa amekwisha kufa; lakini neno wazazi hapa limetumiwa kwa namna nzuri, na linagusia kufahamisha ya kwamba mama wa kambo ana haki ya kuheshimiwa na mtu sawa kama anavyostahili kuheshimiwa mama mzazi. Aya hii pia inaonyesha ya kwamba Yusuf alikwenda nje ya mji kuwalaki wazazi wake.

Mwislamu anapokusudia kutenda jambo, husema, *Inshaa Allah* (Mungu akipenda). Kwa kutumia maneno haya anamwunganisha Allah na nia yake na matendo yake na kumwomba amlinde na maovu. Ni hakika ya kwamba mtu anapomkutanisha Allah na matendo yake si kama atajaribu tu kufanya kazi yake kwa namna impendezayo Mungu, bali pia atazuilika kufikiria maovu.

Aya 101. Kwa kuwa neno *rafa'a* (kunyanyua) pia maana yake ni "kumpeleka mtu mbele

اَحۡسَنَ بِیۡۤ اِذۡ اَخۡرَجَنِیۡ مِنَ السِّجۡنِ وَجَآءَ بِکُمۡ مِّنَ الۡبَدۡوِ مِنۡۢ بَعۡدِ اَنۡ نَّزَغَ الشَّیۡطٰنُ بَیۡنِیۡ وَبَیۡنَ اِخۡوَتِیۡ ؕ اِنَّ رَبِّیۡ لَطِیۡفٌ لِّمَا یَشَآءُ ؕ اِنَّہٗ ہُوَ الۡعَلِیۡمُ الۡحَکِیۡمُ ﴿۱۰۰﴾

Bila shaka Mola wangu Ameifanya kuwa ya kweli. Na Amenifanyia hisani aliponitoa gerezani na kuwaleteni ninyi kutoka jangwani baada ya Shetani kuchochea baina yangu na ndugu zangu. Hakika Mola wangu ni mpole kwa Amtakaye. Bila shaka Yeye ni Mjuzi, Mwenye hekima.

رَبِّ قَدۡ اٰتَیۡتَنِیۡ مِنَ الۡمُلۡکِ وَعَلَّمۡتَنِیۡ مِنۡ تَاۡوِیۡلِ الۡاَحَادِیۡثِ ۚ فَاطِرَ السَّمٰوٰتِ وَالۡاَرۡضِ ۟ اَنۡتَ وَلِیّٖ فِی الدُّنۡیَا وَالۡاٰخِرَۃِ ۚ تَوَفَّنِیۡ مُسۡلِمًا وَّاَلۡحِقۡنِیۡ بِالصّٰلِحِیۡنَ ﴿۱۰۱﴾

102. Ee Mola wangu, Umenibarikia kupata hisa katika ufalme na Ukanifundisha tafsiri ya mambo. Ewe Mwumba wa mbingu na ardhi. Wewe ndiye Rafiki yangu katika dunia na Akhera. Unifishe mnyenyekevu na Uniunganishe na watendao mema.

ذٰلِکَ مِنۡ اَنۡۢبَآءِ الۡغَیۡبِ نُوۡحِیۡہِ اِلَیۡکَ ۚ وَمَا کُنۡتَ لَدَیۡہِمۡ اِذۡ اَجۡمَعُوۡۤا اَمۡرَہُمۡ وَہُمۡ یَمۡکُرُوۡنَ ﴿۱۰۲﴾

103. Hizo ni katika habari za siri Tulizokufunulia. Na hukuwa pamoja nao walipoazimia shauri lao hali wakifanya hila.

وَمَاۤ اَکۡثَرُ النَّاسِ وَلَوۡ حَرَصۡتَ بِمُؤۡمِنِیۡنَ ﴿۱۰۳﴾

104. Na wengi wa watu, hata kama ukipenda, hawatakuwa waaminio.

وَمَا تَسۡـَٔلُہُمۡ عَلَیۡہِ مِنۡ اَجۡرٍ ؕ اِنۡ ہُوَ اِلَّا ذِکۡرٌ لِّلۡعٰلَمِیۡنَ ﴿۱۰۴﴾ ع ۱۱

105. Wala huwaombi ujira juu yake. Huo sio ila ni ukumbusho kwa walimwengu.

---

ya mwenye cheo kikubwa (sura 3:56), Aya hii inaweza kutafsiriwa namna mbili: Kwanza, ya kwamba Yusuf aliwapeleka wazazi wake kwa Mfalme, hivyo neno *'arshi* (kiti) hapa litakuwa na maana ya mfalme. Biblia inasema ya kwamba Yusuf alimpeleka baba yake na baadhi ya nduguze kwa Firauni (Mwanzo 47:2, 7), (Wafalme wa kale wa Misri wakiitwa Firauni). Pili, inaweza kuwa na maana ya kwamba Yusuf aliwakalisha wazee wake juu ya kiti chake cha utawala, maana zamani za kale mawakili wa mfalme walikuwa na viti vyao vya enzi. Hivyo inawezekana ya kwamba Yusuf aliwakalisha wazazi wake na nduguze juu ya kiti chake kwa ruhusa ya Firauni.

Maneno *kharruu lahuu sujjadan* siyo maana yake kuwa wazazi wa Yusuf na nduguze walikwenda sujuda kumsujudia Yusuf. Maana yake ni kwamba walimsujudia Allah kwa ajili ya Yusuf, yaani walimshukuru Mungu kwa kumpa Yusuf cheo kikubwa kama kile. Pia tazama sura 2:35.

Aya 104. Mtume *s.a.w.* anaambiwa hapa ya kuwa ingawa anapenda sana watu waamini, lakini kama ilivyokuwa kwa nduguze Nabii Yusuf, hawataamini mpaka wamwone na mamlaka na utukufu, na wao wenyewe kuaibika na kufedheheka.

FUNGU 12

106. Na Ishara ngapi katika mbingu na ardhi wanazozipita hali wakizipuuza.

وَكَاَيِّنْ مِّنْ اٰيَةٍ فِي السَّمٰوٰتِ وَالْاَرْضِ يَمُرُّوْنَ عَلَيْهَا وَهُمْ عَنْهَا مُعْرِضُوْنَ ﴿١٠٥﴾

107. Na wengi wao hawamwamni Allah isipokuwa huku wanashirikisha.

وَمَا يُؤْمِنُ اَكْثَرُهُمْ بِاللّٰهِ اِلَّا وَهُمْ مُّشْرِكُوْنَ ﴿١٠٦﴾

108. Je, wanajiona salama kuwa hautawafikia msiba wa adhabu ya Allah, au kuwafikia saa ile kwa ghafla na hali hawatambui?

اَفَاَمِنُوْٓا اَنْ تَاْتِيَهُمْ غَاشِيَةٌ مِّنْ عَذَابِ اللّٰهِ اَوْ تَاْتِيَهُمُ السَّاعَةُ بَغْتَةً وَّهُمْ لَا يَشْعُرُوْنَ ﴿١٠٧﴾

109. Sema: Hii ndiyo njia yangu, ninaita kwa Allah. Nipo kwenye busara, mimi na pia wanaonifuata. Na Allah Yu mbali na kila upungufu; wala mimi simo miongoni mwa washirikina.

قُلْ هٰذِهٖ سَبِيْلِيْٓ اَدْعُوْٓا اِلَى اللّٰهِ ۣ عَلٰى بَصِيْرَةٍ اَنَا وَمَنِ اتَّبَعَنِيْ ؕ وَسُبْحٰنَ اللّٰهِ وَمَآ اَنَا مِنَ الْمُشْرِكِيْنَ ﴿١٠٨﴾

110. Na Hatukutuma kabla yako isipokuwa wanaume Tuliowafunulia katika watu wa mji. Je, hawakutembea katika ardhi wakaona jinsi ulivyokuwa mwisho wa wale waliokuwa kabla yao? Na nyumba ya Akhera ni bora kwa wale wamchao; je, hamfahamu?

وَمَآ اَرْسَلْنَا مِنْ قَبْلِكَ اِلَّا رِجَالًا نُّوْحِيْٓ اِلَيْهِمْ مِّنْ اَهْلِ الْقُرٰى ؕ اَفَلَمْ يَسِيْرُوْا فِي الْاَرْضِ فَيَنْظُرُوْا كَيْفَ كَانَ عَاقِبَةُ الَّذِيْنَ مِنْ قَبْلِهِمْ ؕ وَلَدَارُ الْاٰخِرَةِ خَيْرٌ لِّلَّذِيْنَ اتَّقَوْا ؕ اَفَلَا تَعْقِلُوْنَ ﴿١٠٩﴾

111. Hata Mitume walipokata tamaa na (watu) wakadhani kwamba wameambiwa uongo. Msaada Wetu ukawafikia, basi akaokolewa Tuliyemtaka. Na haiondolewi adhabu Yetu kwa watu wakosefu.

حَتّٰٓى اِذَا اسْتَيْـَٔسَ الرُّسُلُ وَظَنُّوْٓا اَنَّهُمْ قَدْ كُذِبُوْا جَآءَهُمْ نَصْرُنَا ۙ فَنُجِّيَ مَنْ نَّشَآءُ ؕ وَلَا يُرَدُّ بَاْسُنَا عَنِ الْقَوْمِ الْمُجْرِمِيْنَ ﴿١١٠﴾

Aya 110. Ni wazi katika Aya hii ya kuwa wanaume tu ndio wanaoweza kuwa Manabii, si wanawake. Lakini fadhili na baraka nyingine za kiroho wanawake na wanaume wote wanaweza kuzifikia.

Aya 111. Mradi wa Aya hii ni kwamba maadui wa Manabii huwa wanazidi sana katika uadui hata unafika wakati Manabii wanafikiri ya kwamba pengine watu wengine hawataamini ghairi ya wale wale waliokwisha amini. Na maadui zao, kwa sababu adhabu ya Allah imekawizwa kuletwa, wanaanza kujiona salama katika kufikiri ya kwamba hakuna adhabu itakayowafikia, na ya kwamba bishara zote walizoambiwa na Manabii ni uwongo mtupu. Mambo

112. Bila shaka katika matukio yao ya kihistoria mna onyo kubwa kwa wenye akili. Si maneno yaliyozushwa, bali ni hakikisho la yale yaliyopo mbele yake, na ni maelezo ya kila kitu, na ni mwongozo na rehema kwa watu wenye kuamini.

لَقَدْ كَانَ فِيْ قَصَصِهِمْ عِبْرَةٌ لِّاُولِي
الْاَلْبَابِ ؕ مَا كَانَ حَدِيْثًا يُّفْتَرٰى وَلٰكِنْ
تَصْدِيْقَ الَّذِيْ بَيْنَ يَدَيْهِ وَتَفْصِيْلَ كُلِّ
شَيْءٍ وَّهُدًى وَّرَحْمَةً لِّقَوْمٍ يُّؤْمِنُوْنَ ﴿۱۱۱﴾ ع ۱۲

---

yanapofikia kiasi hiki, Mungu analeta msaada wake kwa waaminio, na viongozi wa kufuru wanahilikishwa. Haya ndiyo hasa yanayotokea wakati afikapo kila Nabii.

Maneno haya, *Hata Mitume walipokata tamaa,* hayana maana ya kwamba Mitume hukata tamaa ya kufikiwa na msaada wa Mungu. Kufanya ibara ya namna hii ni kosa dhahiri, na inakadhibishwa na Aya 88 ya sura hii hii isemayo, *Hakika hakati tamaa na rehema ya Allah isipokuwa watu makafiri.* Kwa hakika Manabii hawaondoi tamaa ya kusaidiwa na Allah, ila baadhi ya wakati huondoa tamaa juu ya makafiri kuamini, wakati makafiri wanaposhikilia uadui na hawataki kuwasikiliza.

Kadhalika maneno haya, *Wakadhani ya kwamba wameambiwa uwongo,* si maana yake kwamba Manabii ndio walidhani hivyo, bali makafiri. Manabii hawawezi kutia shaka hata kidogo juu ya ukweli wa bishara zao na juu ya ahadi walizopewa na Mungu za kufanikiwa kwao. Imani yao kwa Allah ni isiyotetereka, iliyoko juu ya mwamba wa yakini. Hivyo, waliofikiri kuwa wamedanganywa si Manabii, bali maadui zao waliotajwa katika Aya iliyotangulia.

Aya 112. Aya hii ya mwisho katika sura hii inaeleza ya kwamba mtu akifanya uchunguzi kwa uangalifu wa habari za Manabii wa zamani, utamwongoza kukata shauri ya kwamba Mtume Muhammad kwa hakika ni Mtume wa Mungu; maana si kama anafanana tu na wengi wao, bali bishara za baadhi ya Manabii wa zamani zinatimia katika dhati yake. Kama Mtume ni mwongo, basi hata bishara hizo pia zitakuwa ni za uwongo, kwa sababu kama hazitachukuliwa kwamba zimetimia kwa Mtume Muhammad, basi hakuna mtu mwingine ye yote ziliyemtimilia, hasa kwa vile Ishara zilizotabiriwa kuonekana katika wakati wa Mtume aliyeahidiwa zimekwisha timia. Hii ndiyo shabaha ya maneno, *Ni hakikisho la yale yaliyokuwa kabla yake,* yaliyo katika Aya hii.

Sababu ya pili iliyotolewa katika Aya hii juu ya ukweli wa Mtume Muhammad *s.a.w.* ni kwamba Kitabu alichofunuliwa kinatosheleza kabisa haja na mahitaji ya wanadamu wote, kwa kuwa ni *maelezo ya kila kitu.* Mambo yanapokuwa ni kama hivi, sheria yo yote atakayopewa Mtume mwingine baadaye itafanya kazi gani? Hoja hii inavunja kabisa madai ya mtu ye yote atakayesema amepewa Sheria mpya baada ya Mtume *s.a.w.*

Zaidi ya hayo Qur'an pia ni "mwongozo," yaani, si kama inamwongoza mtu kwenye kweli tu, bali pia inamwongoza katika madaraja yote ya namna mbalimbali ya kukuza tabia zake na roho yake, mpaka imani yake ambayo kwanza ilikuwa juu ya msingi wa akili tu, inavuka kuwa yakini na kujionea mwenyewe hakika yake (tazama sura 1:6). Qur'an inapita hata mbele kuliko hapo, kwa kuwa siyo tu wafuasi wake wanamkaribia Allah, bali pia wanapokea "rehema" Zake na kuona nuru ya Mungu ikiwashukia hasa, na kuona msaada wa Allah unawafikia katika mambo yao yote.

سُوْرَةُ الرَّعْدِ مَكِّيَّةٌ وَّ هِيَ مَعَ الْبَسْمَلَةِ اَرْبَعٌ وَّ اَرْبَعُوْنَ اٰيَةً وَّ سِتَّةُ رُكُوْعَاتٍ

13. SURA AR-RA'D

Imeteremshwa Makka

Ina mafungu 6 na Aya 44 pamoja na Bismillahi

بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ ①

1. Kwa jina la Allah, Mwingi wa rehema, Mwingi wa ukarimu.

الٓمّٓرٰ ۚ تِلْكَ اٰيٰتُ الْكِتٰبِ ؕ وَالَّذِيْٓ
اُنْزِلَ اِلَيْكَ مِنْ رَّبِّكَ الْحَقُّ وَلٰكِنَّ
اَكْثَرَ النَّاسِ لَا يُؤْمِنُوْنَ ②

2. Mimi ni Allah, Nijuaye, Nionaye. Hizi ni Aya za Kitabu. Na yale yaliyoteremshwa kwako kutoka kwa Mola wako ni haki, lakini watu wengi hawaamini.

اَللّٰهُ الَّذِيْ رَفَعَ السَّمٰوٰتِ بِغَيْرِ عَمَدٍ
تَرَوْنَهَا ثُمَّ اسْتَوٰى عَلَى الْعَرْشِ وَسَخَّرَ
الشَّمْسَ وَالْقَمَرَ ؕ كُلٌّ يَّجْرِيْ لِاَجَلٍ
مُّسَمًّى ؕ يُدَبِّرُ الْاَمْرَ يُفَصِّلُ الْاٰيٰتِ
لَعَلَّكُمْ بِلِقَآءِ رَبِّكُمْ تُوْقِنُوْنَ ③

3. Allah Ndiye Aliyeziinua mbingu bila ya nguzo mnazoziona. Kisha Akastawi juu ya Arshi. Na Akavitiisha jua na mwezi; kila kimoja kinaendelea mpaka muda uliowekwa. Yeye Hulitengeneza (kila) jambo. Huzieleza Aya ili mpate yakini ya kukutana na Mola wenu.

Rai yenye nguvu zaidi katika wanazuoni ni ya kwamba sura hii ilishuka Makka. Habari zinazoelezwa ndani yake pia zinatia nguvu rai hii. Juu ya hayo zimo baadhi ya Aya ambazo ushahidi mwingine unaonyesha ya kuwa zilishuka Madina. Aya hizo, asemavyo Ataa, ni ya 44; asemavyo Katada ni ya 32 na wasemavyo wengine ni ya 13 - 15.

Sura hii imeitwa Ra'd (Radi) kwa sababu mvua huja na umeme na radi. Hivyo mvua ya kiroho, yaani wahyi wa Qur'an, pia imekuja na radi na umeme. Uislamu umeleta mapigo ya radi, na watu watakaovuta panga zao ili kuupiga vita, wenyewe wataangamia kwa upanga; na wale wanaoifuata dini inayofundishwa na Qur'an watakalia viti vya enzi ya nguvu na utukufu.

Aya 2. *Alif Laam Miim Raa (Anallahu a'lamu araa)* "Mimi ni Allah, Nijuaye, Nionaye." Mabadiliko katika hizi herufi za mkato yanaonyesha ya kuwa habari zilizomo katika sura hii zimebadilika kidogo. Kujua na kuona kwa Allah ni mbali kabisa na kwa wanadamu. Maneno haya. *Hizi ni Aya za Kitabu,* maana yake ni (a) hizi ni Aya za Kitabu ambacho tabia ya kibinadamu ilikuwa inakingojea; au (b) hizi ni Aya za Kitabu kilichoahidiwa katika Vitabu vya zamani.

Aya 3. *Aliyeziinua mbingu bila ya nguzo mnazoziona*. Maneno haya maana yake ni (1) mnaona ya kuwa mbingu zimesimama bila ya nguzo; au (2) mbingu hazisimami juu ya nguzo zozote mnazoweza kuziona, yaani, zina visimamio vyake lakini hamwezi kuviona. Maana zote hizi mbili ni sahihi na zinapatana na habari zilizomo katika sura yenyewe.

4. Naye ndiye Aliyeitandaza ardhi na Akaweka humo majabali na mito. Na katika kila matunda akafanya humo namna mbili (dume na jike). Huufunika usiku juu ya mchana. Hakika katika hayo zimo Ishara kwa watu wenye kufikiri.

وَهُوَ الَّذِیْ مَدَّ الْاَرْضَ وَجَعَلَ فِیْهَا
رَوَاسِیَ وَاَنْهٰرًا ؕ وَمِنْ كُلِّ الثَّمَرٰتِ جَعَلَ
فِیْهَا زَوْجَیْنِ اثْنَیْنِ یُغْشِی الَّیْلَ النَّهَارَ ؕ
اِنَّ فِیْ ذٰلِكَ لَاٰیٰتٍ لِّقَوْمٍ یَّتَفَكَّرُوْنَ ۝

Aya hii inataka kuondoa fikira za wasioamini kwamba Mtume *s.a.w.* hafanikiwi katika ujumbe wake kwa sababu hana msaada unaoonekana. Aya inasema ya kwamba si lazima kuwa vitu vyote viwe na "nguzo" zionekanazo waziwazi. Mbona mbingu zimesimama kwa miaka isiyojua watu na hazianguki hali hamwoni "nguzo" zake? Basi kazi ya Mtume s.a.w. pia ina "nguzo" ingawa hamzioni, naye ndiye atakayeshinda.

Yeye Hulitengeneza (kila) jambo. Maneno haya pia yanakusudiwa kuonyesha ya kuwa Allah atavifanya vitu vyote viisaidie kazi ya Mtume *s.a.w.* Ulimwengu mzima utamtumikia.

Ili mpate yakini. Yakini ndicho kitu chenye baraka nyingi, kilicho lazima kwa kuokoka. Seyidna Ahmad amesema, "Enyi watu mumtakao Allah! Fungueni masikio na msikie kuwa hapana kitu kama yakini. Yakini peke yake ndiyo humfungua mtu katika madhambi. Yakini ndiyo inayotoa uwezo wa kutenda mema. Na yakini ndiyo imfanyayo mtu ashiki na mpenzi hasa wa Mola wake. Je! mnaweza kuacha dhambi bila yakini? Mnaweza kujikataza matamanio ya nafsi zenu bila nuru ya yakini? Au mnaweza kupata utulivu wa roho bila yakini? Au mnaweza kujibadilisha kweli kweli bila yakini? Je, iko kafara au sadaka yo yote chini ya mbingu yenye kuweza kuwaondoleeni dhambi? Au je damu isiyokuwa ya asili ya Isa mwana wa Mariamu inaweza kuwaokoeni katika madhambi . . . ?

Mtu huondolewa katika madhambi anapomjua kwa yakini Allah na uwezo Wake na malipo Yake. Hakika mzizi wa kila maasi ni ujinga. Mwenye kupata sehemu ya maarifa ya Mungu kwa yakini hawezi kuendelea kumwasi. Mwenye nyumba hawezi kukaa nyumbani mwake akijua kwamba tufani la maji linakuja kwenye welekeo wa nyumba yake; au moto umezunguka nyumba yake na umeiunguza ila pamebakia pahali padogo tu. Basi huyu hawezi kungojea katika nyumba ile. Kwa nini ninyi mmekaa katika hali yenu yenye hatari baada ya kujidai kuwa mna yakini kwa malipo ya Mungu? Basi fumbueni macho yenu na tazameni hukumu za Mungu zilizomo duniani. Na msiwe mapanya waendao chini ya ardhi; bali kuweni njiwa warukao juu na kupenda hewa ya mbinguni. Jihadharini msifanye madhambi baada ya kutubia, wala msiwe kama nyoka mwenye kujichubua gamba lake na ni nyoka vile vile. Yakumbukeni mauti siku zote, kwani yanawasogeleeni pole pole, lakini ninyi mmeghafilika nayo. Jitahidini mtakasike, sababu mtu hawezi kumpata Mtakatifu (Allah) mpaka ajitakase mwenyewe.

Lakini mnawezaje kupata neema hii? Allah amejibu Mwenyewe kama anavyosema katika Qur'an tukufu: Wasta 'iinuu bissabri wassalaat, yaani, Ombeni msaada kwa subira na kwa Sala" (sura 2:46) (Safina ya Nuhu).

وَفِي الْاَرْضِ قِطَعٌ مُّتَجٰوِرٰتٌ وَّجَنّٰتٌ
مِّنْ اَعْنَابٍ وَّزَرْعٌ وَّنَخِيْلٌ صِنْوَانٌ
وَّغَيْرُ صِنْوَانٍ يُّسْقٰى بِمَآءٍ وَّاحِدٍ
وَنُفَضِّلُ بَعْضَهَا عَلٰى بَعْضٍ فِي الْاُكُلِ
اِنَّ فِيْ ذٰلِكَ لَاٰيٰتٍ لِّقَوْمٍ يَّعْقِلُوْنَ ۝٤

5. Na katika ardhi yamo majimbo mbalimbali yaliyoungana, na bustani za mizabibu, na mashamba, na mitende ichipuayo katika shina moja na isiyochipua katika shina moja, vyote vinanyweshelezwa kwa maji yale yale; na Tunaifadhili baadhi yao zaidi kuliko mingine katika matunda. Hakika katika hayo zimo Ishara kwa watu wanaofahamu.

وَاِنْ تَعْجَبْ فَعَجَبٌ قَوْلُهُمْ ءَاِذَا كُنَّا
تُرٰبًا ءَاِنَّا لَفِيْ خَلْقٍ جَدِيْدٍ ؕ اُولٰٓئِكَ
الَّذِيْنَ كَفَرُوْا بِرَبِّهِمْ ۚ وَاُولٰٓئِكَ
الْاَغْلٰلُ فِيْٓ اَعْنَاقِهِمْ ۚ وَاُولٰٓئِكَ
اَصْحٰبُ النَّارِ ۚ هُمْ فِيْهَا خٰلِدُوْنَ ۝٥

6. Na kama ukistaajabu, basi cha ajabu ni usemi wao: Je, tutakapokuwa udongo, kweli tutakuwa katika umbo jipya? Hao ndio waliomkufuru Mola wao, na hao ndio wenye minyororo katika shingo zao, na hao ndio watu wa Motoni, humo watakaa.

وَيَسْتَعْجِلُوْنَكَ بِالسَّيِّئَةِ قَبْلَ الْحَسَنَةِ
وَقَدْ خَلَتْ مِنْ قَبْلِهِمُ الْمَثُلٰتُ ؕ وَاِنَّ
رَبَّكَ لَذُوْ مَغْفِرَةٍ لِّلنَّاسِ عَلٰى ظُلْمِهِمْ ۚ
وَاِنَّ رَبَّكَ لَشَدِيْدُ الْعِقَابِ ۝٦

7. Na wanakuhimiza ulete mabaya kwa haraka kabla ya mema, hali zimekwisha pita adhabu za namna zote kabla yao. Na hakika Mola wako ni Mwenye msamaha kwa watu juu ya dhuluma yao, na hakika Mola wako ni Mkali wa kuadhibu.

وَيَقُوْلُ الَّذِيْنَ كَفَرُوْا لَوْلَآ اُنْزِلَ
عَلَيْهِ اٰيَةٌ مِّنْ رَّبِّهٖ ؕ اِنَّمَآ اَنْتَ مُنْذِرٌ
وَّلِكُلِّ قَوْمٍ هَادٍ ۝٧ ع ٤

8. Na husema wale waliokufuru: Mbona hakuteremshiwa Ishara kutoka kwa Mola wake? Hakika wewe ni Mwonyaji; na kila kaumu ina Kiongozi.

Aya 5. Wasioamini wanaambiwa hapa ya kwamba wasidhani ya kuwa kwa vile Mtume *s.a.w.* ni mtu wa kabila moja nao basi hakuwazidi cho chote. Aya inasema, je, hawaoni ya kuwa vipande vya ardhi vinavyokaribiana vina nguvu namna mbalimbali na vinatoa mazao yanayohitilafiana? Kwa mfano, kipande kimoja kinaotesha namna ya kitu kisichoweza kuoteshwa na kipande cha ardhi kilicho karibu yake. Kadhalika miti ya kabila moja katika bustani moja mara nyingi inapambisha matunda yenye tamu mbalimbali. Basi ni vivyo hivyo kwa wanadamu.

Aya 7. *Mkali wa kuadhibu.* Maneno haya mradi wake ni kuwa adhabu inayotolewa na Allah ni kali zaidi kuliko adhabu inayotolewa na watu.

FUNGU 2

اَللّٰهُ يَعْلَمُ مَا تَحْمِلُ كُلُّ اُنْثٰى وَمَا تَغِيْضُ الْاَرْحَامُ وَمَا تَزْدَادُ ؕ وَكُلُّ شَيْءٍ عِنْدَهٗ بِمِقْدَارٍ ۝٩

9. Allah Anajua abebayo kila mwanamke, na yanavyoviharibu matumbo na yanavyovizidisha. Na kila kitu kiko Kwake kwa kipimo.

عٰلِمُ الْغَيْبِ وَالشَّهَادَةِ الْكَبِيْرُ الْمُتَعَالِ ۝١٠

10. Mjuzi wa siri na dhahiri. Mkuu, Aliye juu.

سَوَآءٌ مِّنْكُمْ مَّنْ اَسَرَّ الْقَوْلَ وَمَنْ جَهَرَ بِهٖ وَمَنْ هُوَ مُسْتَخْفٍۢ بِالَّيْلِ وَسَارِبٌۢ بِالنَّهَارِ ۝١١

11. Ni sawa (Kwake) anayeficha kauli miongoni mwenu na anayeidhihirisha; na (pia) ajifichaye usiku na aendaye mchana.

لَهٗ مُعَقِّبٰتٌ مِّنْۢ بَيْنِ يَدَيْهِ وَمِنْ خَلْفِهٖ يَحْفَظُوْنَهٗ مِنْ اَمْرِ اللّٰهِ ؕ اِنَّ اللّٰهَ لَا يُغَيِّرُ مَا بِقَوْمٍ حَتّٰى يُغَيِّرُوْا مَا بِاَنْفُسِهِمْ ؕ وَاِذَآ اَرَادَ اللّٰهُ بِقَوْمٍ سُوْٓءًا فَلَا مَرَدَّ لَهٗ ۚ وَمَا لَهُمْ مِّنْ دُوْنِهٖ مِنْ وَّالٍ ۝١٢

12. Kwa ajili yake (Mtume) liko kundi (la Malaika) mbele yake na nyuma yake; wanamlinda kwa amri ya Allah. Hakika Allah Habadili yaliyoko kwa watu mpaka wabadili yaliyomo nafsini mwao. Na Allah Anapowatakia watu adhabu, basi hakuna kuizuia, wala hawana mlinzi ye yote badala Yake.

Aya 12. *Liko kundi (la Malaika) mbele yake na nyuma yake.* Yaani, kama vile wafalme hulindwa na askari, kadhalika Mtume *s.a.w.* alikuwa analindwa na kundi la Malaika na pia masahaba wake watawa. Na hii ni kweli. Mara ngapi maadui walitaka kumwua lakini wasifanikiwe!

Kwa mfano, Mtume *s.a.w.* alipokuwa anataka kuhama Makka, ulikuwa ndio wakati makafiri wamefunga shauri kumwendea usiku ili kumwua. Mtume alipokuwa anatoka usiku kwa safari yake ya kuhama, makafiri walikuwa wakija lakini hawakumjua kuwa yeye ndiye Mtume, na wakichelea kuonekana wakajificha, na Mtume *s.a.w.* akapita kwenda zake. Wakakaa nje ya nyumba yake usiku kucha wakimngoja atoke, na asubuhi wakajua kuwa alikwisha ondoka zamani.

Sasa wakaanza kumsaka sana. Mtume *s.a.w.* na Sayidna Abu Bakar walikwenda wakajificha katika pango liitwalo Thaur, mahali pa umbali wa maili tatu au nne kutoka Makka. Usiku ule alikuja buibui akatanda uzi wake na kuuziba mlango wa pango, na njiwa alifika akataga yai pale mlangoni.

Watu wa Makka waliongozwa na fundi wa nyayo mpaka penye pango lile. Yule fundi akawaambia: "Nyayo zimeishia hapa, basi ama wameingia pangoni au wamepaa mbinguni." Mle pangoni Seyidna Abu Bakar akawa na wasiwasi ya kuwa Mtume sasa atakamatwa na kuuawa. Mtume *s.a.w.* akamwambia: "Usihofu wala usihuzunike, hakika Allah yu pamoja nasi."

Wale maadui walimcheka yule fundi wa nyayo kuwa amesema maneno ya ujinga, maana hakuna mtu angeweza kuingia ndani ya pango lile.

Waliposhindwa kumpata, walitangaza ya kuwa mtu atakayemleta Mtume au Abu Bakar wazima au wamekwisha kufa atapata zawadi ya ngamia 100. Zawadi ile ikatangazwa kati ya makabila yaliyokaa kuizunguka Makka.

13. Yeye ndiye Ambaye Huwaonyesheni umeme kwa hofu na tamaa, na Huinua mawingu mazito.

هُوَ الَّذِیْ یُرِیْكُمُ الْبَرْقَ خَوْفًا وَّ طَمَعًا وَّ یُنْشِئُ السَّحَابَ الثِّقَالَ ﴿۱۲﴾

14. Na radi inamsabihi kwa sifa Zake na (pia) Malaika kwa kumhofu; na Hupeleka mapigo ya radi na kumpiga nayo Amtakaye, nao wanabishana juu ya Allah, hali Yeye ni Mkali wa kuadhibu.

وَ یُسَبِّحُ الرَّعْدُ بِحَمْدِهٖ وَ الْمَلٰٓئِكَةُ مِنْ خِیْفَتِهٖ ۚ وَ یُرْسِلُ الصَّوَاعِقَ فَیُصِیْبُ بِهَا مَنْ یَّشَآءُ وَ هُمْ یُجَادِلُوْنَ فِی اللّٰهِ ۚ وَ هُوَ شَدِیْدُ الْمِحَالِ ﴿۱۳﴾

Mkubwa wa Mabedui aitwaye Suraka bin Malik, akashikwa na tamaa ya ngamia 100 na akaondoka kuwafuatia. Akaona mbele yake ngamia wawili wamepandwa. Akajua kuwa ndiyo mawindo yake. Akamchochea farasi wake, lakini farasi alianguka na Suraka akaanguka pamoja naye. Suraka mwenyewe anaeleza tukio hili hivi:-

"Baada ya kuanguka na farasi, nilipiga ramli yangu kwa mshale, kama ilivyokuwa desturi ya kishirikina iliyoenea kati ya Waarabu. Ramli ile ikanikataza. Lakini tamaa ya kupata zawadi ilikuwa kubwa. Nikapanda tena farasi kuwafuata, hata nilikuwa karibu kuwafikia. Mtume alikuwa amepanda kwa heshima, na hakutazama nyuma. Lakini Abu Bakar alikuwa anatazama nyuma mara kwa mara. Niliwakaribia na farasi wangu akakwama tena, nami nikaanguka. Nikapiga ramli tena, ikanikataza. Kwato za farasi zilizama katika mchanga. Kupanda tena ili kuwafuata ikawa vigumu. Nikawapigia kelele nikiwasihi wasimame. Nilipowafikia, nikawaambia nia mbaya niliyokuwa nayo, na ya kwamba moyo wangu umebadilika, na sasa narudi . . ." (Usudul-Ghaaba).

Kwa hakika matokeo ni mengi sana Mtume *s.a.w.* alipolindwa na Allah kwa namna ya ajabu kabisa, hata maadui zake wote wakashindwa kumdhuru mpaka akafanikiwa. Katika ulinzi huu pia inaonekana Mtume Muhammad alikuwa mkubwa kuliko Yesu. Yesu ingawa anasifiwa kuwa mwana wa Mungu, hakulindwa kwa kiasi alicholindwa Mtume Muhammad *s.a.w.* na maadui zake walimshinda kabisa kwa kumtia msalabani, hata hakuthubutu tena baadaye kujionyesha mbele ya adui zake.

Ni wazi ya kuwa kama Mtume *s.a.w*. asingekuwa analindwa na Malaika mbele na nyuma, bila shaka ama angekamatwa wakati wa kutoka nyumbani mwake, au angekamatwa mle pangoni kama maadui wangeinama kidogo tu kuchungulia, au angekamatwa na Suraka na farasi wa Suraka asingeshindwa kwenda. Basi ni hakika ya kuwa ulinzi aliowekewa Mtume na Allah ulikuwa mkubwa kabisa.

Allah Habadili yaliyoko kwa watu mpaka wabadili yaliyomo nafsini mwao. Siyo maana ya maneno haya kwamba Allah hawafanyii ihsani watu wenye dhambi na waovu. Maana yake ni hii tu ya kwamba habadilishi mwendo Wake wa huruma na fadhili kwa watumishi Wake alio-wafadhili kwa sababu ya vitendo vyao vyema, mpaka wao wenyewe wamejibadilisha na kuacha njia ya wema na kushika maovu. Aya hii inaonyesha ya kwamba watu wanapofikiwa na mashaka mfululizo yanayowaangamiza, hiyo ni alama ya wazi ya kwamba wameacha mwendo mwema wa ucha-Mungu.

Katika Aya hii imeelezwa njia moja ya kupata mafanikio na radhi ya Allah. Kama waaminio wakiona wameanguka na kufikiwa na mabalaa, basi wafanye haraka kurejea kwa Allah, na kuacha mwendo wa uovu.

لَهٗ دَعْوَةُ الْحَقِّ ؕ وَالَّذِيْنَ يَدْعُوْنَ مِنْ
دُوْنِهٖ لَا يَسْتَجِيْبُوْنَ لَهُمْ بِشَيْءٍ اِلَّا
كَبَاسِطِ كَفَّيْهِ اِلَى الْمَآءِ لِيَبْلُغَ فَاهُ وَمَا
هُوَ بِبَالِغِهٖ ؕ وَمَا دُعَآءُ الْكٰفِرِيْنَ اِلَّا
فِيْ ضَلٰلٍ ﴿١٥﴾

15. Kwake tu ndiko kunakoelekezwa maombi ya haki. Na wale wanaowaomba badala Yake hawawajibu cho chote, bali (hali yao) ni kama yule anyoshaye mikono yake miwili kwenye maji ili yafike kinywani mwake, lakini hayafikii. Na hayako maombi ya makafiri ila katika upotevu.

وَلِلّٰهِ يَسْجُدُ مَنْ فِي السَّمٰوٰتِ وَالْاَرْضِ
طَوْعًا وَّ كَرْهًا وَّ ظِلٰلُهُمْ بِالْغُدُوِّ
وَالْاٰصَالِ ﴿١٦﴾ ع

16. Na humsujudia Allah waliomo mbinguni na ardhini kwa hiari au kwa karaha, na (pia) vivuli vyao asubuhi na jioni.

قُلْ مَنْ رَّبُّ السَّمٰوٰتِ وَالْاَرْضِ ؕ قُلِ
اللّٰهُ ؕ قُلْ اَفَاتَّخَذْتُمْ مِّنْ دُوْنِهٖۤ اَوْلِيَآءَ لَا
يَمْلِكُوْنَ لِاَنْفُسِهِمْ نَفْعًا وَّلَا ضَرًّا ؕ قُلْ
هَلْ يَسْتَوِي الْاَعْمٰى وَالْبَصِيْرُ ۙ اَمْ هَلْ
تَسْتَوِي الظُّلُمٰتُ وَالنُّوْرُ ۚ اَمْ جَعَلُوْا
لِلّٰهِ شُرَكَآءَ خَلَقُوْا كَخَلْقِهٖ فَتَشَابَهَ
الْخَلْقُ عَلَيْهِمْ ؕ قُلِ اللّٰهُ خَالِقُ كُلِّ شَيْءٍ
وَّهُوَ الْوَاحِدُ الْقَهَّارُ ﴿١٧﴾

17. Sema: Ni nani Mola wa mbingu na ardhi? Sema: Ni Allah. Sema: Je, mnashika walinzi badala Yake, ambao hawamiliki kwa ajili ya nafsi zao manufaa wala dhara? Sema: Je, wanaweza kuwa sawa kipofu na aonaye? Au vinaweza kuwa sawa giza na nuru? Au wamemfanyia Allah washirika ambao wameumba sawa na kuumba Kwake, kwa hiyo viumbe (vya pande mbili) vimeshabihiyana kwao? Sema: Allah ndiye Mwumbaji wa kila kitu, naye ni Mmoja, Mwenye nguvu.

Aya 15. *Al-haq,* "Haki" Neno hili maana yake ni: Kinyume cha batili, yaani ukweli; shauri lililokatwa; adili; kumiliki; kitu kilichoko na kuwepo kwake kunathibitika; yakini; mauti; busara (Akrab).

Kwake ndiyo maombi ya haki. Maneno haya yanaweza kufasiriwa namna nyingi: (1) Mungu tu ndiye anayestahili kuitwa, yaani kuabudiwa; (2) kumwomba Mungu tu ndiko kunakoweza kumfaidia mwanadamu; (3) sauti ya Mungu tu ndiyo inayoinuka kuisaidia haki, yaani mafundisho yaliyo ya kweli na yenye mafao kwa watu, na yasiyo na ubaya hata kidogo wala uwongo, hayaji ila kutoka kwa Mungu; (4) sauti ya Mungu peke yake ndiyo yenye lazima ya kushinda, yaani hakuna awezaye kupindua kusudio la Allah na kumzuia; maana neno haq (haki) pia maana yake ni kitu kinachoshinda na kuimarika.

Maombi ya makafiri. Makafiri wanapoomba miungu ya uwongo, maombi yao yanapotea bure, maana miungu hao hawawezi kuwajibu wala kuwafaa. Lakini hata kafiri akimwomba Mungu, maombi yake yanaweza kukubaliwa na akapewa alichoomba, isipokuwa kama aombe kuwatakia ubaya Manabii na waaminio, hapo hayatakubaliwa.

Aya 17. Qur'an imetumia maneno mawili mbalimbali kueleza Umoja wa Allah:

18. Ameteremsha maji kutoka mawinguni, na mbuga zikapita maji kwa kadiri yao, na furiko la maji likayachukua mapovu yavimbayo. Na katika vile wanavyoyeyusha katika moto kwa kutaka mapambo au vyombo, (huja) povu mfano wake. Hivi ndivyo Allah Hueleza haki na batili. Waama lile povu linapita kama takataka, lakini vile vinavyowafaa watu vinakaa katika ardhi. Hivi ndivyo Allah Hupiga mifano.

اَنْزَلَ مِنَ السَّمَآءِ مَآءً فَسَالَتْ اَوْدِيَةٌۢ
بِقَدَرِهَا فَاحْتَمَلَ السَّيْلُ زَبَدًا رَّابِيًا ؕ وَمِمَّا
يُوْقِدُوْنَ عَلَيْهِ فِى النَّارِ ابْتِغَآءَ حِلْيَةٍ اَوْ
مَتَاعٍ زَبَدٌ مِّثْلُهٗ ؕ كَذٰلِكَ يَضْرِبُ اللّٰهُ
الْحَقَّ وَالْبَاطِلَ ؕ فَاَمَّا الزَّبَدُ فَيَذْهَبُ
جُفَآءً ۚ وَاَمَّا مَا يَنْفَعُ النَّاسَ فَيَمْكُثُ فِى
الْاَرْضِ ؕ كَذٰلِكَ يَضْرِبُ اللّٰهُ
الْاَمْثَالَ ؕ ﴿۱۸﴾

19. Kwa ajili ya wale waliomwitikia Mola wao ni wema; na wale wasiomwitikia, hata kama wangalikuwa na vyote vilivyomo ardhini na (vingine) kama hivyo pamoja navyo, bila shaka wangalivitoa kujikombolea. Hao watakuwa na hesabu mbaya, na makao yao ni Jahanamu, na ni mahali pabaya palioje!

لِلَّذِيْنَ اسْتَجَابُوْا لِرَبِّهِمُ الْحُسْنٰى ؕ
وَالَّذِيْنَ لَمْ يَسْتَجِيْبُوْا لَهٗ لَوْ اَنَّ لَهُمْ مَّا فِى
الْاَرْضِ جَمِيْعًا وَّمِثْلَهٗ مَعَهٗ لَافْتَدَوْا بِهٖ ؕ
اُولٰٓئِكَ لَهُمْ سُوْٓءُ الْحِسَابِ ۙ وَمَاْوٰىهُمْ
جَهَنَّمُ ؕ وَبِئْسَ الْمِهَادُ ﴿۱۹﴾ ع

(1) Ahad na (2) Waahid. Neno la kwanza maana yake ni Umoja halisi wa Allah bila kuhusiana na kitu cho chote. Neno la pili maana yake ni "Wa kwanza" au "Chanzo".

Aya 18. Katika Aya hii mifano miwili imeelezwa. Katika mfano wa kwanza haki inafananishwa na maji, na uwongo unafananishwa na povu. Mwanzoni uwongo unaonekana kama utaishinda haki, lakini mwishoni unaondolewa kama vile takataka zinavyosukumwa na mkondo wenye nguvu wa maji. Katika mfano wa pili, haki inafananishwa na dhahabu au fedha ambayo ikiyeyushwa inatoa povu la takataka ambalo hutupwa na kuacha dhahabu au fedha iliyo safi.

Maana ya methali hii ni kwamba nguvu ya Uislamu lazima itaondoa povu la dini za uwongo na desturi mbaya. Methali hii pia maana yake ni kwamba wanapofika Mitume wa Mungu, kuzindukana kunatokea katika jinsi ya mwanadamu kunakoleta mashindano kati ya maelekeo yake mema na mila mbaya anazozifuata. Watu ambao jinsi yao ni njema wanatoka ndani ya mashindano hayo hali maoni yao yenye makosa yamebadilika kwa maoni yaliyo sawa.

Aya 19. Aya hii inasema ya kwamba watu wanaowakubali Mitume wa Mungu na kuitikia wito wa Allah, mwishoni watafanikiwa na watakutana na Mola wao. Akili zao zitatiwa nguvu na zitakuwa kali na zenye nuru. Lakini wale wanaokataa wito Wake wataendelea kuanguka polepole mpaka kushindwa na maangamio vitawafunikiza, na hakuna fidia au ukombozi utakaowaokoa katika adhabu ya Mungu.

FUNGU 3

20. Je, anayejua ya kwamba yaliyoteremshwa kwako kutoka kwa Mola wako ni haki, ni kama aliye kipofu? Wenye akili tu ndiyo wenye kushika nasaha:

اَفَمَنْ يَّعْلَمُ اَنَّمَاۤ اُنْزِلَ اِلَيْكَ مِنْ رَّبِّكَ الْحَقُّ كَمَنْ هُوَ اَعْمٰى ؕ اِنَّمَا يَتَذَكَّرُ اُولُوا الْاَلْبَابِ ۙ﴿۱۹﴾

21. Ambao hutimiza ahadi ya Allah wala hawavunji mapatano;

الَّذِيْنَ يُوْفُوْنَ بِعَهْدِ اللّٰهِ وَلَا يَنْقُضُوْنَ الْمِيْثَاقَ ۙ﴿۲۰﴾

22. Na ambao huunganisha Aliyoyaamuru Allah yaunganishwe, na humwogopa Mola wao, na huiogopa hesabu mbaya;

وَالَّذِيْنَ يَصِلُوْنَ مَاۤ اَمَرَ اللّٰهُ بِهٖۤ اَنْ يُّوْصَلَ وَيَخْشَوْنَ رَبَّهُمْ وَيَخَافُوْنَ سُوْٓءَ الْحِسَابِ ؕ﴿۲۱﴾

23. Na ambao husubiri kwa kutaka radhi ya Mola wao, na wakasimamisha Sala na wakatoa katika vile Tulivyowapą kwa siri na dhahiri, na kuyaondoa maov kwa wema, hao ndiyo watapata malipo (mema) ya nyumba (ya Akhera).

وَالَّذِيْنَ صَبَرُوا ابْتِغَآءَ وَجْهِ رَبِّهِمْ وَاَقَامُوا الصَّلٰوةَ وَاَنْفَقُوْا مِمَّا رَزَقْنٰهُمْ سِرًّا وَّعَلَانِيَةً وَّيَدْرَءُوْنَ بِالْحَسَنَةِ السَّيِّئَةَ اُولٰٓئِكَ لَهُمْ عُقْبَى الدَّارِ ۙ﴿۲۲﴾

Aya 21-22. Katika Aya hizi mbili mpaka Aya 23 zimetajwa alama za watu wenye akili ambao wametajwa mwisho wa Aya 20. Aya 22 inaonyesha ya kuwa wenye akili wanapokwisha timiza ahadi yao kwa Allah, na kujiunganisha naye kwa mwungano wa kweli na ulio halisi, basi wanageukia viumbe Wake na kujiunganisha nao mwungano wa kweli. Hivyo baada ya kutimiza wajibu walio nao kwa Allah, pia wanatimiza wajibu walio nao kwa viumbe Wake, na kwa kutimiza kazi hizi mbili wanatumia njia zilizoumbwa na Allah.

Na humwogopa Mola wao. Maana ya maneno haya ni kwamba wenye akili wanapokwisha kufungamana na Allah sawasawa, daima wanakaa katika hadhari na kuogopa isije ufungamano huo ukavunjika kwa ajili ya makosa yao.

Hivyo Aya 22 inaonyesha ya kwamba watu wenye akili ni waangalifu na wenye wasiwasi wakiogopa wasifukuzwe kuwa karibu na Allah baada ya kuwa wamekwisha mfikia, na upande mwingine wanaogopa wasimkasirishe Allah kwa kukosa kuwatimizia viumbe wenzao haki zao.

Aya 23. *Wakasimamisha Sala.* Mtume s.a.w amesema: "Hakika kila Sala inafuta hatia zilizoitangulia." "Jambo la kwanza litakalohesabiwa siku ya Kiyama ni Sala za faradhi," "Baina ya mtu na kufuru ni kuacha Sala" (Kashful-Ghummah). Pia tazama sura 2:4.

Seyidna Ahmad (Amani ya Mungu juu yake) ameandika, Sala ni nini? Sala ni dua inayoombwa kwa Mungu kwa unyenyekevu na kwa kumsifu na kumtukuza na kumwomba msamaha na kumsalia Mtume *s.a.w.* Kwa hivi, ninyi mnaposali Sala zenu msiombe dua zenu kwa maneno ya Kiarabu tu kama watu wenye kughafilika; kwani Sala zao na kutubia kwao hakuna maana. Lakini ninyi mnaposali si vibaya kuomba dua zenu kwa unyenyekevu katika lugha zenu,

24. Bustani za milele. Wataziingia wao na waliofanya wema miongoni mwa baba zao na wake wao na wazao wao. Na Malaika watawajia kupitia kila mlango.

جَنّٰتُ عَدْنٍ يَّدْخُلُوْنَهَا وَمَنْ صَلَحَ مِنْ اٰبَآئِهِمْ وَاَزْوَاجِهِمْ وَذُرِّيّٰتِهِمْ وَالْمَلٰٓئِكَةُ يَدْخُلُوْنَ عَلَيْهِمْ مِّنْ كُلِّ بَابٍ ﴿٢٤﴾

25. Iwe amani juu yenu, kwa sababu mlisubiri; basi ni mema yaliyoje matokeo ya nyumba (ya Akhera)!

سَلٰمٌ عَلَيْكُمْ بِمَا صَبَرْتُمْ فَنِعْمَ عُقْبَى الدَّارِ ﴿٢٥﴾

26. Na wale wanaovunja ahadi ya Allah baada ya kuifunga, na wanakata Aliyoyaamuru Allah yaunganishwe, na wanafanya uharibifu katika nchi; hao ndio watapata laana, na watapata nyumba mbaya.

وَالَّذِيْنَ يَنْقُضُوْنَ عَهْدَ اللّٰهِ مِنْۢ بَعْدِ مِيْثَاقِهٖ وَيَقْطَعُوْنَ مَآ اَمَرَ اللّٰهُ بِهٖٓ اَنْ يُّوْصَلَ وَيُفْسِدُوْنَ فِى الْاَرْضِ ۙ اُولٰٓئِكَ لَهُمُ اللَّعْنَةُ وَلَهُمْ سُوْٓءُ الدَّارِ ﴿٢٦﴾

27. Allah Hukunjua riziki kwa Amtakaye na Hudhikisha. Na wamefurahia maisha ya dunia, hali maisha ya dunia mbele ya Akhera ni starehe ndogo tu.

اَللّٰهُ يَبْسُطُ الرِّزْقَ لِمَنْ يَّشَآءُ وَيَقْدِرُ ۙ وَفَرِحُوْا بِالْحَيٰوةِ الدُّنْيَا ۗ وَمَا الْحَيٰوةُ الدُّنْيَا فِى الْاٰخِرَةِ اِلَّا مَتَاعٌ ﴿٢٧﴾

---

isipokuwa Qur'an ambayo ni maneno ya Mungu na dua zilizobainishwa katika Hadithi ambazo ni maneno ya Mtume s.a.w. ili athari ya kuomba na unyenyekevu iwe katika mioyo yenu.

Kuyaondoa maovu kwa wema. Katika maneno haya zimeelezwa njia za kuondoa maovu. (1) Waaminio wanafanya vitendo vizuri na kufanya wema ili watu waige mfano wao na kuacha maovu; (2) Wanawapa watu maagizo ya wema kila mara, na hawaingii sana katika kueleza habari za maovu; (3) Wanatenda vitendo vizuri kama vinavyohitajiwa na nyakati. Inapokuwa kuadhibu na kutoa kisasi ndiko kutaleta wema, basi wataadhibu; au wakiona kuwa kusamehe ndiko kutaleta wema, basi wanasamehe. Mwendo wao si wa kulipiza kisasi tu kama ifundishavyo Taurati, wala si wa kusamehe tu kama ifundishavyo Injili; bali wao wanashika mwendo wa katikati, wakifanya kila jambo kwa kuangalia kuwa ndilo lenye kufaa katika wakati huo, na litaleta wema; (4) Uovu na machafuko yanayoletwa na watu hayawachochei nao kufanya machafuko na uovu, bali kila mara wanakuwa waadilifu.

'Uqba-d-daar. "Malipo (mema) ya nyumba (ya Akhera)." Neno 'uqba-d-daar maana yake ni mwisho; hali ya mwisho; matokeo; malipo au thawabu au tuzo (Akrab).

Aya 25. *Kwa sababu mlisubiri.* Waaminio watapata amani inayodumu kama alivyosema Allah, ni kwa sababu walisubiri; yaani walivumilia misiba na mateso na wakadumu kufuata Sheria. Aya hii pia inaonyesha ya kuwa watu wanaokata tamaa na kubabaika wanapofikiwa na misiba, wao hawawezi kupata amani na salama, na hawastahili kupata Pepo.

FUNGU 4

28. Na wanasema wale waliokufuru: Kwa nini hakuteremshiwa Ishara kutoka kwa Mola wake? Sema: Hakika Allah Humwangamiza Amtakaye na Humwongoza Kwake anayeelekea.

وَيَقُوْلُ الَّذِيْنَ كَفَرُوْا لَوْلَآ اُنْزِلَ عَلَيْهِ
اٰيَةٌ مِّنْ رَّبِّهٖ ؕ قُلْ اِنَّ اللّٰهَ يُضِلُّ مَنْ يَّشَآءُ
وَيَهْدِيْٓ اِلَيْهِ مَنْ اَنَابَ ۚ﴿۲۸﴾

29. Wale walioamini na ikatulia mioyo yao kwa kumkumbuka Allah. Sikilizeni! Kwa kumkumbuka Allah mioyo hutulia.

اَلَّذِيْنَ اٰمَنُوْا وَتَطْمَئِنُّ قُلُوْبُهُمْ بِذِكْرِ
اللّٰهِ ؕ اَلَا بِذِكْرِ اللّٰهِ تَطْمَئِنُّ الْقُلُوْبُ ﴿۲۹﴾

30. Wale walioamini na kufanya vitendo vizuri, raha itakuwa yao, na marudio mema.

اَلَّذِيْنَ اٰمَنُوْا وَعَمِلُوا الصّٰلِحٰتِ طُوْبٰى
لَهُمْ وَحُسْنُ مَاٰبٍ ﴿۳۰﴾

31. Kama hivyo Tumekutuma katika watu ambao wamekwisha pita kabla yao watu wengine, ili uwasomee Tunayokufunulia, na wao wanamkufuru Rahmani. Sema: Yeye ndiye Mola wangu, hakuna aabudiwaye ila Yeye; nimemtegemea na marejeo yangu ni Kwake.

كَذٰلِكَ اَرْسَلْنٰكَ فِيْٓ اُمَّةٍ قَدْ خَلَتْ
مِنْ قَبْلِهَآ اُمَمٌ لِّتَتْلُوَا عَلَيْهِمُ الَّذِيْٓ
اَوْحَيْنَآ اِلَيْكَ وَهُمْ يَكْفُرُوْنَ
بِالرَّحْمٰنِ ؕ قُلْ هُوَ رَبِّيْ لَآ اِلٰهَ اِلَّا هُوَ ۚ
عَلَيْهِ تَوَكَّلْتُ وَاِلَيْهِ مَتَابِ ﴿۳۰﴾

32. Na kama ingalikuwako Qur'an ambayo kwayo milima ingalisafirishwa, au kwayo ardhi ingalipasuliwa, au wafu wangalisemeshwa kwayo (je, wangaliikubali?) Bali Shauri lote ni kwa Allah. Je, hawajajua walioamini ya kwamba Allah Angalipenda bila shaka Angaliwaongoza watu wote? Wala msiba hautaacha kuwafikia wale waliokufuru

وَلَوْ اَنَّ قُرْاٰنًا سُيِّرَتْ بِهِ الْجِبَالُ اَوْ
قُطِّعَتْ بِهِ الْاَرْضُ اَوْ كُلِّمَ بِهِ الْمَوْتٰى ؕ
بَلْ لِّلّٰهِ الْاَمْرُ جَمِيْعًا ؕ اَفَلَمْ يَايْئَسِ
الَّذِيْنَ اٰمَنُوْٓا اَنْ لَّوْ يَشَآءُ اللّٰهُ لَهَدَى
النَّاسَ جَمِيْعًا ؕ وَلَا يَزَالُ الَّذِيْنَ كَفَرُوْا

Aya 29. Kama vile watu wa kidunia kadiri wanavyopata kitu kidogo wanatamani wapate zaidi, kadhalika watu wanaomtafuta Mungu, kadiri wanavyomwelekea ndivyo nyoyo zao zinavyozidi kupata utulivu.

Aya 32. *Aljiibal,* "Milima." Neno hili ni wingi wa neno *jabal* (mlima). Neno *jabal*

kwa sababu ya yale waliyoyafanya au utashuka karibu na nyumba zao mpaka ifike ahadi ya Allah. Hakika Allah Havunji miadi.

تُصِيْبُهُمْ بِمَا صَنَعُوْا قَارِعَةٌ اَوْ تَحُلُّ
قَرِيْبًا مِّنْ دَارِهِمْ حَتّٰى يَاْتِيَ وَعْدُ اللّٰهِ ؕ
اِنَّ اللّٰهَ لَا يُخْلِفُ الْمِيْعَادَ ۝٣١ ع

FUNGU 5

33. Na kwa yakini Mitume walifanyiwa mzaha kabla yako, lakini Niliwapa nafasi wale waliokufuru, kisha Nikawakamata. Basi ilikuwaje adhabu Yangu!

وَلَقَدِ اسْتُهْزِئَ بِرُسُلٍ مِّنْ قَبْلِكَ
فَاَمْلَيْتُ لِلَّذِيْنَ كَفَرُوْا ثُمَّ اَخَذْتُهُمْ ۫
فَكَيْفَ كَانَ عِقَابِ ۝٣٢

---

hutumiwa kwa mfano kwa maana ya (1) mkubwa wa watu au wa kabila; (2) mwanachuoni anayewazidi wenziwe; (3) taabu kubwa au msiba (Akrab).

Aya hii haionyeshi kuwa Qur'an haina sifa ya kung'oa milima na kupasua ardhi na kuwasemesha wafu. Bali mradi wake ni kuwa hata kama sifa hizo za Qur'an zingewadhihirikia makafiri, hata hivyo wasingeamini.

Ambayo kwayo milima ingalisafirishwa. Maana ya maneno haya ni kwamba Qur'an ina bishara za kutokea matetemeko ya nchi yenye kutisha na yenye nguvu, yatakayoing'oa milima. Kwa hakika inatabiri misukosuko mikubwa katika dunia hii (soma sura 99).

Neno "milima" lina maana ya taabu kubwa na mashaka. Kwa maana hii Aya hii inaonyesha jambo ambalo ni hakika ya kuwa Qur'an inatatua matatanisho yote ya mambo ya siasa za utawala, makao ya watu, mambo ya mali na iktisadi, mambo ya tabia zilizo bora na mambo ya kiroho, kwa namna isiyofanywa na dini nyingine yo yote.

Neno "milima" pia lina maana ya "wanazuoni" au "wakubwa." Kwa maana hii maelezo ya Aya hii yanahusiana na Qur'an; maana ilipofika, viongozi wa watu wa zamani na wanazuoni wao wakatoweka. Taratibu za serikali zikabadilika kabisa, na usultani uliorithika ukabadilishwa kwa ukhalifa, yaani serikali inayotawaliwa na mtu anayechaguliwa na watu wenyewe. Elimu za kizamani za ushirikina na hofu za upuuzi zikaondolewa na elimu za kujua mambo kwa kuyapima na kuyajaribu kwa kuchungua na kuelewa tabia za vitu. Qur'an imejaa Aya zinazowahimiza watu watumie akili na kufikiri badala ya kushughulika na fikira za kishirikina, na inawahimiza wachungue kwa uangalifu kanuni za asili. Qur'an inasema, dunia yote imeumbwa kwa ajili ya kumfaa mwanadamu, na hivyo mwanadamu anahimizwa mara kwa mara kuulazimisha ulimwengu umtumikie. Kwa kifupi, Qur'an ilitangua kanuni za taratibu za zamani na kuweka namna mpya za kuangalia shida za wanadamu.

Maneno haya, *Kwayo nchi ingalipasuliwa,* yanaonyesha ya kuwa Qur'an itaenea upesi duniani. Pia maana yake ni kuwa baadhi ya ardhi za maadui zitaingia mikononi mwa Waislamu, na haya yote mawili yalitimia kama ilivyotabiri Qur'an, maana ilienea upesi sana dunia nzima, na nchi nzima-nzima zikaingia katika milki za Waislamu.

Wafu wangalisemeshwa kwayo. Yaani, mababu wacha-Mungu wa vizazi vilivyopita washuhudie ukweli wa Qur'an kuwa imetoka kwa Mungu, kama walivyoshuhudia wacha-Mungu waliopita zamani katika Vitabu vya Biblia. Pia wafu kuzungumza mradi wake ni kwamba watokee ndani ya ndoto na kuwaambia watu ukweli wa Mtume wa Mungu. Haya yote yalitokea. Kadhalika neno "wafu" linaweza kuwa na maana ya watu waliokufa kiroho, kama linavyopatikana neno hili kwa maana hii katika sura 8:25.

34. Je, Aliye Msimamizi juu ya kila nafsi kwa yale iliyoyachuma (Hatawauliza)? Na wakamfanyia Allah washirika. Sema: Watajeni. Au mtamwambia Asiyoyajua katika ardhi, au ni maneno matupu? Bali wamepambiwa waliokufuru hila zao na wakazuiliwa njia (ya haki). Na ambaye Allah Anamwacha kupotea, basi yeye hana mwongozi.

اَفَمَنۡ هُوَ قَآئِمٌ عَلٰى كُلِّ نَفۡسٍۢ بِمَا كَسَبَتۡ ؕ وَجَعَلُوۡا لِلّٰهِ شُرَكَآءَ ؕ قُلۡ سَمُّوۡهُمۡ ؕ اَمۡ تُنَبِّـُٔوۡنَهٗ بِمَا لَا يَعۡلَمُ فِى الۡاَرۡضِ اَمۡ بِظَاهِرٍ مِّنَ الۡقَوۡلِ ؕ بَلۡ زُيِّنَ لِلَّذِيۡنَ كَفَرُوۡا مَكۡرُهُمۡ وَصُدُّوۡا عَنِ السَّبِيۡلِ ؕ وَمَنۡ يُّضۡلِلِ اللّٰهُ فَمَا لَهٗ مِنۡ هَادٍ ۝٣٣

35. Wanayo adhabu katika maisha ya dunia; na bila shaka adhabu ya Akhera ni ngumu zaidi; wala hawatakuwa na yeyote wa kuwaokoa kwa Allah.

لَهُمۡ عَذَابٌ فِى الۡحَيٰوةِ الدُّنۡيَا وَلَعَذَابُ الۡاٰخِرَةِ اَشَقُّ ۚ وَمَا لَهُمۡ مِّنَ اللّٰهِ مِنۡ وَّاقٍ ۝٣٤

36. (Huu ni) mfano wa Pepo waliyoahidiwa wamchao; chini yake hutiririka mito, matunda yake ni ya daima na (pia) kivuli chake. Huu ndiyo mwisho wa wale wamchao Mungu, na mwisho wa makafiri ni Moto.

مَثَلُ الۡجَنَّةِ الَّتِىۡ وُعِدَ الۡمُتَّقُوۡنَ ؕ تَجۡرِىۡ مِنۡ تَحۡتِهَا الۡاَنۡهٰرُ ؕ اُكُلُهَا دَآئِمٌ وَّظِلُّهَا ؕ تِلۡكَ عُقۡبَى الَّذِيۡنَ اتَّقَوۡا ۖ وَّعُقۡبَى الۡكٰفِرِيۡنَ النَّارُ ۝٣٥

Aya 34. *Watajeni.* Maneno haya yana hoja yenye nguvu ya kubatilisha *shirk.* Waabudu-masanamu wanaambiwa kueleza ni kazi gani zinazofanywa na miungu wao. Neno "Watajeni" katika Aya hii si maana yake kutaja majina ya miungu ya masanamu bali kutaja majina ya sifa zao, kwani majina ya baadhi ya hao waungu yametajwa ndani ya Qur'an yenyewe, na si kwamba hayajulikani (tazama sura 71:24). Kuwataka waabudu masanamu waeleze kazi zinazofanywa na masanamu yao ni jambo ambalo lazima litawahakikishia ujinga wao wanaoufanya.

Kadhalika neno, *Watajeni,* linaweza kuwa neno la dharau kwa maana ya kwamba miungu wa makafiri ni hafifu mno hata kuwataja tu kunatosha kuwafedhehesha makafiri.

Maneno haya, *Au (je) mtamwambia Asiyoyajua katika ardhi,* yana hoja nyingine yenye nguvu inayobatilisha *shirk.* Aya inahoji ya kwamba kama kungekuwako waungu wengine, Mungu Mwenyewe ilikuwa lazima ajulishe jambo hilo kwa watu kwa kumwambia Mtume Wake au *Malaika* Zake, au hao washirika wenyewe wangetangaza jambo hilo; lakini hakuna tangazo lo lote la namna hiyo au ujumbe kama huo unaojulikana umepata kuwepo duniani. Hivyo Aya inawarudi waabudu mizimu kwa kuwaambia ya kwamba wanapomwekea Allah washirika ni kama wanataka kumfahamisha Allah jambo ambalo Yeye Mwenyewe halijui.

Maneno haya, *Au ni maneno matupu?,* maana yake ni kwamba waabudu-masanamu wanasema mambo haya kwa ndimi zao tu na hawayaamini kweli kweli. Aya inawauliza makafiri kama ni kwa hakika wanayaamini wanayoyasema?

Aya 36. *Matunda yake ni ya daima na (pia) kivuli chake.* Maneno haya yanaonyesha ya

37. Na ambao Tuliwapa Kitabu, wanafurahia uliyoteremshiwa. Na katika makundi wako wanaoyakataa baadhi yake. Sema: Nimeamrishwa kumwabudu Allah tu wala nisimshirikishe. Ninaita Kwake, na Kwake ni marudio yangu.

وَالَّذِيْنَ اٰتَيْنٰهُمُ الْكِتٰبَ يَفْرَحُوْنَ بِمَآ اُنْزِلَ اِلَيْكَ وَمِنَ الْاَحْزَابِ مَنْ يُّنْكِرُ بَعْضَهٗ ؕ قُلْ اِنَّمَآ اُمِرْتُ اَنْ اَعْبُدَ اللّٰهَ وَلَآ اُشْرِكَ بِهٖ ؕ اِلَيْهِ اَدْعُوْا وَ اِلَيْهِ مَاٰبِ ﴿۳۷﴾

38. Na hivyo Tukaiteremsha hukumu iliyo wazi. Na kama ukifuata matamanio yao baada ya kukufikia elimu, hutakuwa na rafiki wala mlinzi mbele ya Allah.

وَكَذٰلِكَ اَنْزَلْنٰهُ حُكْمًا عَرَبِيًّا ؕ وَلَئِنِ اتَّبَعْتَ اَهْوَآءَهُمْ بَعْدَ مَا جَآءَكَ مِنَ الْعِلْمِ ۙ مَالَكَ مِنَ اللّٰهِ مِنْ وَّلِيٍّ وَّلَا وَاقٍ ﴿۳۸﴾ ع ۱۱

FUNGU 6

39. Na bila shaka Tuliwatuma Mitume kabla yako, na Tukawapa wake na watoto. Na haiyumkiniki Mtume kuleta Ishara isipokuwa kwa idhini ya Allah. Kila muda unayo hukumu iliyoandikwa.

وَلَقَدْ اَرْسَلْنَا رُسُلًا مِّنْ قَبْلِكَ وَجَعَلْنَا لَهُمْ اَزْوَاجًا وَّذُرِّيَّةً ؕ وَمَا كَانَ لِرَسُوْلٍ اَنْ يَّاْتِيَ بِاٰيَةٍ اِلَّا بِاِذْنِ اللّٰهِ ؕ لِكُلِّ اَجَلٍ كِتَابٌ ﴿۳۹﴾

40. Allah Huyafuta Ayatakayo na Huyaimarisha Ayatakayo, na asili ya hukumu iko Kwake.

يَمْحُوا اللّٰهُ مَا يَشَآءُ وَيُثْبِتُ ۚ وَعِنْدَهٗٓ اُمُّ الْكِتٰبِ ﴿۴۰﴾

41. Na kama Tukikuonyesha baadhi ya Tuliyowaahidi, au Tukikufisha, basi juu yako ni kufikisha tu, na juu yetu ni kuhesabu.

وَاِنْ مَّا نُرِيَنَّكَ بَعْضَ الَّذِيْ نَعِدُهُمْ اَوْ نَتَوَفَّيَنَّكَ فَاِنَّمَا عَلَيْكَ الْبَلٰغُ وَعَلَيْنَا الْحِسَابُ ﴿۴۱﴾

kwamba matunda ya Peponi hayatakuwa na msimu, na hivyo neema hizo hazikatiki. "Matunda" na "kivuli" ni maneno mawili yanayoashiria neema za ndani na za nje, na kuonyesha ya kwamba waaminio watapata namna zote za starehe huko Peponi, za nje na za ndani.

Aya 37. *Ahzaab*, "Makundi" mradi wake ni makundi ya watu hao wote ambao walipelekewa Mtume lakini wasimkubali. Katika Aya hii watu wanaosemwa ni Mayahudi, Wakristo na wasioamini wengine, kwa vile Mtume s.a.w. ametumwa kwa watu wote wa duniani.

Aya 40. Aya hii imeweka sheria mbili zinazohusiana na adhabu: (a) Mungu huondoa adhabu sehemu au yote; (b) anaiacha ifanyike kama ilivyokadiriwa. Hivyo adhabu haiji kamwe mpaka imestahili, wala haizidi kosa, ingawa inaweza kuwa ndogo kuliko ilivyostahili, au inaweza kuachwa kabisa, Kanuni hii haibadiliki katika adhabu zote za Allah.

42. Je, hawakuona ya kwamba Tunaifikia ardhi Tukiipunguza mipaka yake? Na Allah Huhukumu; hakuna wa kuibadili hukumu Yake. Naye ni Mwepesi wa kuhesabu.

اَوَلَمۡ يَرَوۡا اَنَّا نَاۡتِى الۡاَرۡضَ نَنۡقُصُهَا
مِنۡ اَطۡرَافِهَا ؕ وَاللّٰهُ يَحۡكُمُ لَا مُعَقِّبَ
لِحُكۡمِهٖ ؕ وَهُوَ سَرِيۡعُ الۡحِسَابِ ﴿۴۲﴾

43. Na wamekwisha fanya hila wale waliokuwa kabla yao, lakini hila zote ni za Allah. Anajua inayoyachuma kila nafsi; na hivi karibuni makafiri watajua matokeo (mema) ya nyumba (ya Akhera) ni kwa ajili ya nani?

وَقَدۡ مَكَرَ الَّذِيۡنَ مِنۡ قَبۡلِهِمۡ فَلِلّٰهِ
الۡمَكۡرُ جَمِيۡعًا ؕ يَعۡلَمُ مَا تَكۡسِبُ
كُلُّ نَفۡسٍ ؕ وَسَيَعۡلَمُ الۡكُفّٰرُ لِمَنۡ
عُقۡبَى الدَّارِ ﴿۴۳﴾

44. Na wanasema waliokufuru: Wewe si Mtume. Sema: Allah Anatosha kuwa Shahidi baina yangu na baina yenu, na (pia) yule mwenye elimu ya Kitabu.

وَيَقُوۡلُ الَّذِيۡنَ كَفَرُوۡا لَسۡتَ مُرۡسَلًا ؕ
قُلۡ كَفٰى بِاللّٰهِ شَهِيۡدًا بَيۡنِىۡ وَبَيۡنَكُمۡ ۙ
وَمَنۡ عِنۡدَهٗ عِلۡمُ الۡكِتٰبِ ﴿۴۴﴾ ع ۱۴

Aya 42. Aya hii inawavunja kabisa hao wanaoleta ubishi juu ya Mtume *s.a.w.* wakisema kuwa hakuonyesha Ishara. Aya inasema, je, hawaoni ya kwamba Allah anaipunguza ardhi toka kila upande? Je, hii siyo Ishara ya kushinda kwa Uislamu? Uislamu unaingia kila nyumba na kila mahali na katika watu wa aina zote - wakubwa na wadogo, matajiri na maskini, mtumwa na bwana. Je, hii siyo Ishara ya kutosha kuwafahamisha wote wenye nia safi?

Neno *ardh* (ardhi) pia linaweza kuwa na maana ya "nchi ya Bara Arabu." Katika hali hiyo Aya italeta maana ya kwamba Uislamu utaenea haraka katika nchi nzima ya Bara Arabu. Neno *Atallaahu* kwa matumizi ya Kiarabu pia maana yake ni Allah kufika pamoja na adhabu (tazama sura 2:211 na 16:27).

Aya 44. Mtume s.a.w. anaambiwa asichukie au kupata wasiwasi kwamba watu hawaamini ingawa Ishara nyingi zimeonyeshwa. Ana haja gani ya kupata wasiwasi hali anao mashahidi wawili - Ishara mpya-mpya zitokazo kwa Allah na bishara za kufika kwake zilizomo katika Vitabu vilivyotangulia? Ndiyo maana Mungu anamaliza sura hii kwa kusema: *Allah Anatosha kuwa Shahidi . . . na (pia) yule mwenye elimu ya Kitabu.*

سُوْرَةُ اِبْرَاهِيْمَ مَكِّيَّةٌ وَّهِيَ مَعَ الْبَسْمَلَةِ ثَلَاثٌ وَّخَمْسُوْنَ اٰيَةً وَّسَبْعَةُ رُكُوْعَاتٍ

14. SURA IBRAHIIM

Imeteremshwa Makka

Ina mafungu 7 na Aya 53 pamoja na Bismillahi

بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ ①

1. Kwa jina la Allah, Mwingi wa rehema, Mwingi wa ukarimu.

الٓرٰ ۟ كِتٰبٌ اَنْزَلْنٰهُ اِلَيْكَ لِتُخْرِجَ النَّاسَ مِنَ الظُّلُمٰتِ اِلَى النُّوْرِ ۙ بِاِذْنِ رَبِّهِمْ اِلٰى صِرَاطِ الْعَزِيْزِ الْحَمِيْدِ ۙ ②

2. Mimi ni Allah Nionaye. (Hiki ni) Kitabu Tumekiteremsha kwako ili uwatoe watu katika giza kuwapeleka kwenye nuru, kwa ruhusa ya Mola wao, mpaka kwenye njia ya Ashindaye, Asifiwaye-

اللّٰهِ الَّذِيْ لَهٗ مَا فِي السَّمٰوٰتِ وَمَا فِي الْاَرْضِ ؕ وَوَيْلٌ لِّلْكٰفِرِيْنَ مِنْ عَذَابٍ شَدِيْدِ ۙ ③

3. Allah; Ambaye ni Vyake vilivyomo katika mbingu na vilivyomo katika ardhi. Na ole kwa makafiri kwa adhabu iliyo kali.

الَّذِيْنَ يَسْتَحِبُّوْنَ الْحَيٰوةَ الدُّنْيَا عَلَى الْاٰخِرَةِ وَيَصُدُّوْنَ عَنْ سَبِيْلِ اللّٰهِ وَيَبْغُوْنَهَا عِوَجًا ؕ اُولٰٓئِكَ فِيْ ضَلٰلٍۢ بَعِيْدٍ ④

4. Wale wanaopenda maisha ya dunia kuliko Akhera, na kuzuilia (watu) njia ya Allah, na wanataka kuipotosha. Hao wamo katika upotevu wa mbali.

Sura hii yote ilishuka Makka. Ibni Abbas na Katada wanasema ya kuwa Aya 29-31 zilishuka Madina.

Aya 2. *Alif Laam Raa*. (Tazama sura 2:2; 10:2 na 13:2).

Aya hii inaonyesha kuwa Qur'an ni "nuru" ambayo Mtume s.a.w. anaitumia kwa kuwaongoza watu kuwatoa gizani kuwapeleka katika nuru ambayo ni "njia ya Ashindaye, Asifiwaye." Sifa ya "Ashindaye" inahusu nuru ya nje, na sifa ya "Asifiwaye" inahusu nuru ya ndani ya moyo. Mtu anayejikuzia sifa ya kwanza anapewa uwezo wa kuwashinda maadui zake wa nje, na anasalimika na dhara na taabu za kiwiliwili, ambapo yule anayekuza nafsini mwake sifa ya pili anapata uwezo wa kumshinda adui yake wa ndani, yaani Shetani, na anajiondolea giza la shaka, ujinga, kukata tamaa na mawazo mabaya. Waarabu kwa kumfuata Mtume s.a.w. walitoka katika giza za namna zote hizo mbili. Waliacha ushirikina, ujinga, kuabudu masanamu na mwendo mchafu waliokuwa nao. Kadhalika wakawa wafalme na wenye kumiliki mamlaka makubwa na wakawa waalimu waliofundisha dini ulimwenguni.

Aya 4. *Wanataka kuipotosha.* Maana ya maneno haya ni kwamba. Ingawa kwa nje wanadai kuwa wanatafuta mwongozo, lakini ndani yao ni watu wapotofu, na hawataki kuachilia mbali njia mbovu za wazee wao. Hapo matokeo yanakuwa kwamba, kwa kutaka kuridhi dhamiri

5. Na Hatukumtuma Mtume ye yote isipokuwa kwa lugha ya watu wake ili kuwabainishia. Kisha Allah Anamwacha kupotea Amtakaye, na kumwongoza Amtakaye. Naye ni Mwenye nguvu, Mwenye hekima.

وَمَآ اَرْسَلْنَا مِنْ رَّسُوْلٍ اِلَّا بِلِسَانِ
قَوْمِهٖ لِيُبَيِّنَ لَهُمْ ؕ فَيُضِلُّ اللّٰهُ مَنْ
يَّشَآءُ وَيَهْدِيْ مَنْ يَّشَآءُ ؕ وَهُوَ
الْعَزِيْزُ الْحَكِيْمُ ۝٤

6. Na bila shaka Tulimtuma Musa pamoja na Ishara Zetu: ya kwamba watoe watu wako katika giza kuwapeleka kwenye nuru, na uwakumbushe siku za Allah. Bila shaka katika hayo zimo Ishara kwa kila avumiliaye sana, anayeshukuru.

وَلَقَدْ اَرْسَلْنَا مُوْسٰى بِاٰيٰتِنَآ اَنْ اَخْرِجْ
قَوْمَكَ مِنَ الظُّلُمٰتِ اِلَى النُّوْرِ ۙ
وَذَكِّرْهُمْ بِاَيّٰىمِ اللّٰهِ ؕ اِنَّ فِيْ ذٰلِكَ
لَاٰيٰتٍ لِّكُلِّ صَبَّارٍ شَكُوْرٍ ۝٥

---

zao zenye wasiwasi, wanaita desturi walizotengeneza wenyewe kuwa dini ya Mungu. Kujiridhi huku kwa uwongo kunawakosesha wao na wafuasi wao kupata mwongozo wa kweli.

Aya 5. Si mradi wa Aya hii kwamba Mjumbe wa Allah apokee ufunuo wake katika lugha ya watu wa kabila lake tu. Mradi wake ni kuwa sehemu kubwa ya ufunuo wake lazima iwe katika lugha ya watu wake ili wale wanaopokea kwanza ufunuo wake wasipate shida. Hutokea Mtume apokee ufunuo katika lugha ya watu wa nchi nyingine. Kwa hakika ufunuo huo wa namna ya pekee huwa ni mwujiza.

Ni kosa kufasiri Aya hii kama walivyofasiri baadhi ya waandishi wa Kikristo kuwa Mtume *s.a.w.* alitumwa kwa Waarabu tu. Tafsiri ya namna hii inakanushwa kabisa na Qur'an yenyewe ambayo inasema Mtume *s.a.w*. alitumwa kwa dunia nzima (sura 7:159 na 34:29). Si Qur'an tu inayodai kuwa Mtume *s.a.w*. alitumwa kwa dunia yote, bali Mtume mwenyewe alidai kuwa ametumwa kwa ajili ya dunia nzima. Kwa mfano alisema: *Bu'ithtu ilal aswadi wal ahmari,* yaani, "Nimetumwa kwa watu weusi na watu wekundu," yaani kwa dunia nzima (Bihar). Tena alisema, *Bu'ithtu ilannaasi 'aammah,* yaani "Nimetumwa kwa wanadamu wote" (Bukhari). Tena akasema, *Ursiltu ilal khalqi kaaffah,* yaani, "Nimetumwa kwa viumbe wote" (Mishkat).

Undani wa Aya hii unahakikisha ya kwamba lugha ya Kiarabu ndiyo iliyozaa lugha zote, kwa sababu ya kwamba kwa vile Mtume Muhammad *s.a.w.* ametumwa kwa dunia nzima, lugha ambayo Allah aliifanya itumike kuletea ujumbe aliokuja nao lazima iwe kwa namna yo yote iliyozaa lugha zote za dunia. Jambo hili limehakikishwa kabisa kuwa ni kweli na Seyidna Ahmad, Mwanzilishi wa Mwendeleo wa Uislamu wa Ahmadiyya, katika kitabu chake kiitwacho *Minanur-Rahmaan.*

Aya 6. *Siku za Allah* ni siku ambazo Allah aliwasaidia waaminio juu ya maadui zao, kadhalika siku za Allah ni siku alizowaadhibu maadui za Manabii kwa sababu ya uovu wao. Aya hii inaonyesha ya kwamba njia nzuri ya kuwatoa watu gizani ni kwa kuwakumbusha fadhili na adhabu za Allah.

Katika maneno haya, *Bila shaka katika hayo zimo Ishara kwa kila avumiliaye sana, anayeshukuru.* Waislamu wanaonywa ya kwamba watajaribiwa kama walivyojaribiwa wafuasi wa Musa kwa kupitishwa katika misukosuko, na ni pale tu watakapovumilia taabu zote na kutoka ndani yake bila imani yao kupata doa, basi hapo watazirithi fadhili za Allah. Lakini wakionekana hawana shukrani kama walivyokuwa watu wa Nabii Musa, basi watatiwa katika adhabu.

7. Na (kumbuka) aliposema Musa kwa watu wake: Kumbukeni neema ya Allah iliyo juu yenu, Alipowaokoeni kwa watu wa Firauni, waliowapeni adhabu mbaya, na wakawachinja wana wenu na wakaacha hai wanawake wenu. Na katika hayo ilikuwa jaribio kubwa kutoka kwa Mola wenu.

وَاِذْ قَالَ مُوْسٰى لِقَوْمِهِ اذْكُرُوْا نِعْمَةَ
اللّٰهِ عَلَيْكُمْ اِذْ اَنْجٰىكُمْ مِّنْ اٰلِ فِرْعَوْنَ
يَسُوْمُوْنَكُمْ سُوْٓءَ الْعَذَابِ وَيُذَبِّحُوْنَ
اَبْنَآءَكُمْ وَيَسْتَحْيُوْنَ نِسَآءَكُمْ ؕ وَفِيْ
ذٰلِكُمْ بَلَآءٌ مِّنْ رَّبِّكُمْ عَظِيْمٌ ۝٦ ع

FUNGU 2

8. Na (kumbukeni) Alipotangaza Mola wenu: Kama mkishukuru, bila shaka Nitawazidishieni, na kama mkikufuru, (jueni) hakika adhabu Yangu ni kali sana.

وَاِذْ تَاَذَّنَ رَبُّكُمْ لَئِنْ شَكَرْتُمْ
لَاَزِيْدَنَّكُمْ وَلَئِنْ كَفَرْتُمْ
اِنَّ عَذَابِيْ لَشَدِيْدٌ ۝٧

9. Na Musa akasema: Kama mtakufuru ninyi na waliomo ardhini wote, basi hakika Allah ni Ajitoshaye kabisa, Asifiwaye.

وَقَالَ مُوْسٰٓى اِنْ تَكْفُرُوْٓا اَنْتُمْ وَمَنْ فِي
الْاَرْضِ جَمِيْعًا ۙ فَاِنَّ اللّٰهَ لَغَنِيٌّ حَمِيْدٌ ۝٨

10. Je, hazikuwafikieni habari za wale wa kabla yenu, watu wa Nuhu na Waadi na Wathamudi, na wale wa baada yao? Hakuna awajuaye ila Allah.

اَلَمْ يَاْتِكُمْ نَبَؤُا الَّذِيْنَ مِنْ قَبْلِكُمْ
قَوْمِ نُوْحٍ وَّعَادٍ وَّثَمُوْدَ ۛؕ وَالَّذِيْنَ مِنْۢ
بَعْدِهِمْ ۛؕ لَا يَعْلَمُهُمْ اِلَّا اللّٰهُ ؕ جَآءَتْهُمْ
رُسُلُهُمْ بِالْبَيِّنٰتِ فَرَدُّوْٓا اَيْدِيَهُمْ فِيْٓ

Aya 8. Shukrani ni namna tatu: (1) Shukrani ya moyo au ya akili, ambayo ni mtu kufahamu kwa kiasi cha kutosha fadhili alizofadhiliwa; (2) shukrani ya ulimi, ambayo ni kumsifu na kumshangilia aliyekufadhili; (3) kushukuru kwa viungo, yaani kuitumia faida uliyopata kama inavyofaa. Shukrani huwa juu ya misingi mitano: (a) Anayetoa shukrani anyenyekee kwa yule anayemshukuru; (b) ampende; (c) aseme kuwa amefaidishwa na fadhili aliyotendewa; (d) amsifu kwa sababu ya kumfadhili; (e) asitumie alichopewa kwa namna inayoweza kumchukiza aliyekitoa. Hii ndiyo Shukrani kwa upande wa mwanadamu.

Shukrani atoayo Allah kumpa mtu ni kumsamehe, kumkubalia au kuridhika naye, kumwandalia heri na fadhili, kumtukuza na kumpa malipo mema.

Aya hii inaeleza kanuni kubwa ya kwamba maendeleo ya kila namna yamefungamana na *shukr* (shukurani). Yaani Allah Mwenye huruma amekadiria ya kwamba vipawa alivyompa mwanadamu vizidi anapovitumia vizuri. Kwa mfano, kama mtu ataitumia vizuri elimu lazima itazidi. Kadhalika kama viungo vya mwili vitatumiwa vizuri, lazima vitapata nguvu zaidi. Hii kanuni ya Allah ya rehema Yake inafanya kazi katika watu wote wa kila kabila, wa kila rangi na wa kila dini. Kanuni hii inafanya kazi katika mambo yote - ya dini na ya kidunia.

Aya 10. Maneno ya Qur'an ya *faradduu aidiyahum fii af-wahihim* (wakarudisha mikono

اَفْوَاهِهِمْ وَقَالُوْٓا اِنَّا كَفَرْنَا بِمَآ اُرْسِلْتُمْ بِهٖ وَاِنَّا لَفِيْ شَكٍّ مِّمَّا تَدْعُوْنَنَآ اِلَيْهِ مُرِيْبٍ ۝٩

Waliwafikia Mitume wao kwa Ishara waziwazi, ndipo wakarudisha mikono yao juu ya vinywa vyao, na wakasema: Hakika sisi tunayakataa mliyotumwa nayo, na sisi tunayo shaka ihangaishayo kwa hayo mnayotuitia.

قَالَتْ رُسُلُهُمْ اَفِي اللّٰهِ شَكٌّ فَاطِرِ السَّمٰوٰتِ وَالْاَرْضِ ؕ يَدْعُوْكُمْ لِيَغْفِرَ لَكُمْ مِّنْ ذُنُوْبِكُمْ وَيُؤَخِّرَكُمْ اِلٰٓى اَجَلٍ مُّسَمًّى ؕ قَالُوْٓا اِنْ اَنْتُمْ اِلَّا بَشَرٌ مِّثْلُنَا ؕ تُرِيْدُوْنَ اَنْ تَصُدُّوْنَا عَمَّا كَانَ يَعْبُدُ اٰبَآؤُنَا فَاْتُوْنَا بِسُلْطٰنٍ مُّبِيْنٍ ۝١٠

11. Mitume wao wakasema: Je, Mnamfanyia Allah shaka, Mwumba wa mbingu na ardhi? Yeye Anawaiteni ili kuwasameheni dhambi zenu na kuwapeni muhula mpaka muda uliowekwa. Wakasema: Ninyi sio ila ni watu kama sisi, mnataka kutuzuilia waliyokuwa wakiabudu baba zetu. Basi tuleteeni dalili iliyo wazi.

قَالَتْ لَهُمْ رُسُلُهُمْ اِنْ نَّحْنُ اِلَّا بَشَرٌ مِّثْلُكُمْ وَلٰكِنَّ اللّٰهَ يَمُنُّ عَلٰى مَنْ يَّشَآءُ مِنْ عِبَادِهٖ ؕ وَمَا كَانَ لَنَآ اَنْ نَّاْتِيَكُمْ بِسُلْطٰنٍ اِلَّا بِاِذْنِ اللّٰهِ ؕ وَعَلَى اللّٰهِ فَلْيَتَوَكَّلِ الْمُؤْمِنُوْنَ ۝١١

12. Mitume wao wakawaambia: Sisi sio ila ni watu kama ninyi; lakini Allah Humfanyia hisani Amtakaye katika watumishi Wake. Wala sisi hatuwezi kuwaleteeni dalili isipokuwa kwa ruhusa ya Allah. Na kwa Allah wategemee waaminio.

---

yao juu ya vinywa vyao) yanachora picha ya mtu anayeweka mkono wake juu ya kinywa chake akiashiria kukifunga. Kabla ya kuyaelezea amaneno haya maalum, ni lazima mtu aamue pia ni nani anayerejewa katika Aya hii. Ni dhahiri kwamba kitendo hiki kinanasibishwa kwa makafiri; kwa hiyo kinaweza kutafsiriwa kwa namna mbili. Kinaweza kutafsiriwa kwamba hao, makafiri, walipeleka mikono yao kwa nguvu na kwa haraka vinywani mwao wao wenyewe. Hii ina maana kwamba walikataa kuwa na mazungumzo yo yote na Manabii na wafuasi wao. Hatua hii inafikiwa wakati hatimae mtu anafadhaika na anabakiwa hana hoja yo yote. Kwa hiyo anajitwalia msimamo huu wa kususia, ikiashiria kwamba hana cha kusema zaidi.

Katika tafsiri ya pili ile rejea yaweza kuwa inavihusu vinywa vya Manabii. Hiyo pia inaonyesha kukatika kule kule kwa mazungumzo lakini kwa njia tofauti. Kwa hiyo ujumbe utakuwa kwamba hatimae makafiri wanawazuia Manabii wasihubiri zaidi kwa kuwaambia wafunge vinywa vyao. Tafsiri hii ya pili inaungwa mkono zaidi na sehemu iliyobakia ya aya hii ambapo makafiri wanaeendelea kuipanua zaidi hoja hii kwa kusema' "Tumeyakataa mliyotumwa nayo na hakika sisi tunayo shaka ihangaishayo kuhusu hayo mnayotuitia."

Aya 11. *Faatiri-s-samaawaat,* "Mwumba wa mbingu." Maneno haya maana yake ni Mwumba au Mwanzishaji wa mbingu. Ibni Abbas anasema, "Sikuwa najua maana ya *faatiri-s-samaawaat* mpaka Waarabu wawili wa jangwani walipofika kwangu wakigombania kisima, na mmoja akasema, *Anaa aftartuhaa,* yaani, "Mimi ndiye nilikianzisha."

13. Na tuna nini tusimtegemee Allah na hali Ametuonyesha njia zetu? Na kwa yakini tutayavumilia mnayotuudhi. Basi kwa Allah wategemee wategemeao.

وَمَا لَنَآ اَلَّا نَتَوَكَّلَ عَلَى اللّٰهِ وَقَدْ هَدٰىنَا سُبُلَنَا ؕ وَلَنَصْبِرَنَّ عَلٰى مَآ اٰذَيْتُمُوْنَا ؕ وَعَلَى اللّٰهِ فَلْيَتَوَكَّلِ الْمُتَوَكِّلُوْنَ ﴿١٣﴾ ع ٢

FUNGU 3

14. Na wale waliokufuru wakawaambia Mitume wao: Kwa yakini tutawatoeni katika nchi yetu au lazima mtarudi katika mila yetu. Basi Mola wao Akawafunulia: Bila shaka Tutawaangamiza wadhalimu.

وَقَالَ الَّذِيْنَ كَفَرُوْا لِرُسُلِهِمْ لَنُخْرِجَنَّكُمْ مِّنْ اَرْضِنَآ اَوْ لَتَعُوْدُنَّ فِيْ مِلَّتِنَا ؕ فَاَوْحٰٓى اِلَيْهِمْ رَبُّهُمْ لَنُهْلِكَنَّ الظّٰلِمِيْنَ ﴿١٤﴾

15. Na kwa yakini Tutawakalisheni katika nchi baada yao. Hii ni kwa yule Aliyeogopa cheo Changu na akaogopa onyo Langu.

وَلَنُسْكِنَنَّكُمُ الْاَرْضَ مِنْۢ بَعْدِهِمْ ؕ ذٰلِكَ لِمَنْ خَافَ مَقَامِيْ وَخَافَ وَعِيْدِ ﴿١٥﴾

16. Na wakaomba ushindi, na akashindwa kila jabari, adui ya haki.

وَاسْتَفْتَحُوْا وَخَابَ كُلُّ جَبَّارٍ عَنِيْدٍ ﴿١٦﴾

Katika Qur'an inaonekana ya kwamba kuna madaraja manne ya kuumba: (a) Daraja ambalo kulipokuwa hakuna cho chote, na kazi ya kuumba ikaanza kwa mara ya kwanza, hali hakukuwa cho chote kilichokuwapo kabla ya wakati huo; (b) daraja ambalo vitu vilipodhihirika, lakini kabla havijawa na umbo lo lote halisi; (c) daraja ambalo vitu kwa kuchanganyika na kuunganika vikaanza kuwa na tabia, au hali na sifa namna mbalimbali; kukamilika kwa kazi hiyo ikawa ndiyo kawaida ya asili; na (d) daraja la mwisho ni ilipoanza kazi ya kuzaana na kuumba kukafanyika tena na tena, yaani, mtu akazaa mtu na mbegu ikazaa mbegu n.k.w. Sifa ya *Faatir* inahusu daraja la pili la hayo manne.

Aya 13. *Tutayavumilia mnayotuudhi*. Maneno haya yanaonyesha jinsi Manabii wa Allah wanavyokiri unyonge wao. Hawadai ya kwamba wana nguvu kuwazidi maadui zao, bali wanakubali ya kuwa maadui zao wana zana nyingi za kidunia na wanaweza kupata taabu nyingi kwao kama Allah asiwasaidie. Lakini kwa kuwa wanafanya kazi yao kwa amri ya Mungu, watalazimika kuvumilia mateso yote kwa subira, na jambo hili litahakikisha ya kwamba hawakuwa na nia ya kujitukuza wenyewe kwa kuwaita watu kuwafuata . Na kwa kuwa tegemeo lao ni kwa Allah, walijua pia ya kuwa wao ndio watashinda mwishoni.

Aya 15. *Hii ni kwa yule aliyeogopa cheo Changu na akaogopa onyo Langu.* Maneno haya yanaonyesha bayana ya kuwa ahadi ya ushindi wamepewa wale tu wanaoukiri na kuukubali utukufu wa Allah na uwezo Wake, na wanaamini ya kuwa Allah ndiye Mmiliki wa siku ya Kiyama, na ambao wanaogopa isije dhambi zao zikawateremshia adhabu ya Allah.

مِّنۡ وَّرَآىِٕهٖ جَهَنَّمُ وَ يُسۡقٰى مِنۡ
مَّآءٍ صَدِيۡدٍ ۙ﴿۱۷﴾

17. Nyuma yake iko Jahanamu na atanyweshwa maji yaliyochemka.

يَّتَجَرَّعُهٗ وَلَا يَكَادُ يُسِيۡغُهٗ وَيَاۡتِيۡهِ
الۡمَوۡتُ مِنۡ كُلِّ مَكَانٍ وَّمَا هُوَ بِمَيِّتٍ ؕ
وَمِنۡ وَّرَآىِٕهٖ عَذَابٌ غَلِيۡظٌ ﴿۱۸﴾

18. Atayanywa kidogo kidogo wala hataweza kuyameza kwa urahisi. Na mauti yatamfikia kutoka kila mahali, hata hivyo hatakufa. Na zaidi ya hayo itakuwako adhabu kali kwa ajili yake.

مَثَلُ الَّذِيۡنَ كَفَرُوۡا بِرَبِّهِمۡ اَعۡمَالُهُمۡ
كَرَمَادِ ِۨاشۡتَدَّتۡ بِهِ الرِّيۡحُ فِىۡ يَوۡمٍ
عَاصِفٍ ؕ لَا يَقۡدِرُوۡنَ مِمَّا كَسَبُوۡا
عَلٰى شَىۡءٍ ؕ ذٰلِكَ هُوَ الضَّلٰلُ الۡبَعِيۡدُ ﴿۱۹﴾

19. Mfano wa wale waliomkufuru Mola wao: vitendo vyao ni kama majivu unayoyapeperusha kwa nguvu upepo katika siku ya kimbunga. Hawatakuwa na uwezo juu ya cho chote walichokichuma. Huo ndio upotevu wa mbali.

اَلَمۡ تَرَ اَنَّ اللّٰهَ خَلَقَ السَّمٰوٰتِ وَالۡاَرۡضَ
بِالۡحَقِّ ؕ اِنۡ يَّشَاۡ يُذۡهِبۡكُمۡ وَ يَاۡتِ
بِخَلۡقٍ جَدِيۡدٍ ۙ﴿۲۰﴾

20. Je, huoni kwamba Allah Amezi-umba mbingu na ardhi kwa haki? Kama Akipenda Atawaondoeni na kuleta vi-umbe wapya.

وَّمَا ذٰلِكَ عَلَى اللّٰهِ بِعَزِيۡزٍ ﴿۲۱﴾

21. Na hilo kwa Allah si gumu.

وَبَرَزُوۡا لِلّٰهِ جَمِيۡعًا فَقَالَ الضُّعَفٰٓؤُا
لِلَّذِيۡنَ اسۡتَكۡبَرُوۡۤا اِنَّا كُنَّا لَكُمۡ تَبَعًا
فَهَلۡ اَنۡتُمۡ مُّغۡنُوۡنَ عَنَّا مِنۡ عَذَابِ اللّٰهِ
مِنۡ شَىۡءٍ ؕ قَالُوۡا لَوۡ هَدٰٮنَا اللّٰهُ
لَهَدَيۡنٰكُمۡ ؕ سَوَآءٌ عَلَيۡنَاۤ اَجَزِعۡنَاۤ اَمۡ
صَبَرۡنَا مَا لَنَا مِنۡ مَّحِيۡصٍ ﴿۲۲﴾ ع ۱۳

22. Na wote watahudhuria kwa Allah; ndipo wanyonge watasema kuwaambia wale waliojivuna: Hakika sisi tulikuwa tukiwafuateni ninyi, basi je, ninyi mnaweza kutuondolea cho chote katika adhabu ya Allah? Watasema: Angalituongoza Allah bila shaka tungaliwaongozeni. (Lakini sasa) ni mamoja kwetu tusiposubiri au tukisubiri, hatuna pa kukimbilia.

Imani kama hiyo ni lazima iweko kwa watu ili wapate kutimiziwa ahadi ya kupata msaada wa Allah. Hili linaonyesha ya kwamba kuukubali Uislamu kwa jina tu hakutoshi kwa ajili ya kupata ushindi na mafanikio.

Aya 19. *Waliomkufuru Mola wao.* Maneno haya si maana yake kuwa wanakataa kuwapo kwa Allah, kwani hata waabudu masanamu wa Makka waliamini kuwa Mungu yuko. Maana ya maneno haya ni kwamba wanakataa neema au mamlaka ya Allah. Wako hata katika hao wanaoitwa wataalamu watu ambao wanamwamini Allah, lakini hawaamini kuwa Mungu ana haja ya kujiingiza katika habari za dunia hii. Matendo ya watu kama

FUNGU 4

وَقَالَ الشَّيْطٰنُ لَمَّا قُضِيَ الْاَمْرُ اِنَّ اللّٰهَ
وَعَدَكُمْ وَعْدَ الْحَقِّ وَوَعَدْتُّكُمْ
فَاَخْلَفْتُكُمْ ؕ وَمَا كَانَ لِيَ عَلَيْكُمْ مِّنْ
سُلْطٰنٍ اِلَّاۤ اَنْ دَعَوْتُكُمْ فَاسْتَجَبْتُمْ
لِيْ ۚ فَلَا تَلُوْمُوْنِيْ وَلُوْمُوْۤا اَنْفُسَكُمْ ؕ
مَاۤ اَنَا بِمُصْرِخِكُمْ وَمَاۤ اَنْتُمْ
بِمُصْرِخِيَّ ؕ اِنِّيْ كَفَرْتُ بِمَاۤ
اَشْرَكْتُمُوْنِ مِنْ قَبْلُ ؕ اِنَّ الظّٰلِمِيْنَ
لَهُمْ عَذَابٌ اَلِيْمٌ ﴿۲۲﴾

23. Na Shetani atasema itakapokatwa shauri: Hakika Allah Aliwaahidini ahadi ya kweli, nami niliwaahidini lakini sikuwatimizieni. Wala sikuwa na mamlaka juu yenu isipokuwa niliwaiteni nanyi mkaniitikia. Basi msinilaumu, bali jilaumuni wenyewe: siwezi kuwasaidieni, wala ninyi hamwezi kunisaidia. Hakika mimi nilikataa kunishirikisha kwenu toka zamani. Kwa yakini wadhalimu watakuwa na adhabu iumizayo.

وَاُدْخِلَ الَّذِيْنَ اٰمَنُوْا وَعَمِلُوا الصّٰلِحٰتِ
جَنّٰتٍ تَجْرِيْ مِنْ تَحْتِهَا الْاَنْهٰرُ
خٰلِدِيْنَ فِيْهَا بِاِذْنِ رَبِّهِمْ ؕ تَحِيَّتُهُمْ فِيْهَا
سَلٰمٌ ﴿۲۳﴾

24. Na wataingizwa wale walioamini na kufanya vitendo vizuri katika Mabustani yapitayo mito ndani yao, wakikaa humo kwa idhini ya Mola wao. Maamkio yao humo yatakuwa, Salaam.

hao yamekuwa wakfu kwa ajili ya kuendeleza mambo yao ya kidunia tu. Hawana fikra yo yote juu ya Allah, na hawafanyi cho chote ili kumpendeza Mungu. Basi ni matendo ya watu kama hao yanayosemwa na Aya hii kuwa hayana maana na yanapotea bure, na hayatakuwa na thawabu katika Akhera. Matendo yao yamefanana na majivu yanayopeperushwa na upepo mkali na yakasambazwa ovyo.

Maneno "vitendo vyao" pia yanaweza kuwa na maana ya juhudi zinazofanywa na maadui wa Manabii wa Mungu ya kwamba hazitaleta matokeo yo yote na zitakufa bure. Badala ya kuwaletea makusudio wanayoyataka kwa vitendo hivyo, vinawaletea adhabu ya kuhiliki na kuangamia itokayo kwa Allah.

Aya 23. *Siwezi kuwasaidieni.* Kwa kusema maneno haya Shetani anaonyesha kuwa hana uwezo wo wote wa kuwapoteza watu. Na ni kweli hana uwezo huo. Yeye ni chombo tu cha kudhihirisha udhaifu wa mwanadamu kama vile Malaika walivyo kwa kudhihirisha sifa njema za mwanadamu. Kwa hakika mtu hupotezwa na matamanio yake mabaya, kama inavyosema Aya hii, Shetani huita tu na mtu mwenyewe akaitikia. Kama asingeitika, dhara yo yote isingemgusa. Kazi ya Shetani ni kuwapa watu mashauri mabaya na mtu anakuwa na hiyari kuyafuata au kuyakataa. Kadhalika kazi ya Malaika ni kuwapa watu mashauri mema waliyo na hiyari kuyafuata au kuyaacha. Malaika hawawezi kumfanya mtu kuwa mwema, wala Shetani hawezi kumfanya mtu kuwa mbaya. Wao huonyesha njia tu, nzuri au mbaya, na yaliyobakia ni kazi ya mwanadamu mwenyewe.

Ni ajabu ya kwamba Shetani anasema, kama isemavyo Aya hii, ya kwamba alikataa kushirikishwa na Mungu toka zamani. Katika maana moja, hii ni kweli; maana aliyeona utukufu wa Mungu hawezi kufanya kosa la *shirk* la kuweka waungu wengine pamoja na Allah. Katika hali hii Shetani anaweza kufananishwa na dawa ya nusu-kaputi. Kabla nusu-kaputi haijaingia

25. Je, hukuona jinsi Allah Alivyopiga mfano wa neno zuri? Ni kama mti mzuri (ambao) mzizi wake ni imara na (kila) tawi lake lafika mbinguni.

اَلَمۡ تَرَ كَيۡفَ ضَرَبَ اللّٰهُ مَثَلًا كَلِمَةً طَيِّبَةً كَشَجَرَةٍ طَيِّبَةٍ اَصۡلُهَا ثَابِتٌ وَّفَرۡعُهَا فِى السَّمَآءِ ﴿۲۴﴾

26. Hutoa matunda yake kila wakati kwa idhini ya Mola wake. Na Allah Huwapigia watu mifano ili washike nasaha.

تُؤۡتِىۡۤ اُكُلَهَا كُلَّ حِيۡنٍۢ بِاِذۡنِ رَبِّهَا ؕ وَيَضۡرِبُ اللّٰهُ الۡاَمۡثَالَ لِلنَّاسِ لَعَلَّهُمۡ يَتَذَكَّرُوۡنَ ﴿۲۵﴾

---

mwilini ni dawa yenye maana sana; lakini inapotumiwa vibaya inakuwa sumu inayoua kabisa. Hivyo kabla Shetani hajapenya katika roho ya mtu anakuwa ni kitu cha vivi hivi. Hakika Shetani ni wakili aliyewekwa kudhihirisha udhaifu wa binadamu.

Aya 25 na **26.** Aya hizi ni kubwa kabisa katika Qur'an. Aya hizi zina kanuni zisizoweza kukosa zinazomsaidia mtu kutambua ukweli wa Kitabu kilichoteremshwa na Allah kinachodai kutosheleza haja na mahitaji ya wanadamu wote.

Katika Aya hii neno la Mungu limefananishwa na mti wenye sifa tano:

(1) *Tayyib*, wenye umbo zuri la kupendeza. Hivyo kitabu cha Mungu kinatakiwa kisiwe hata kidogo na mafundisho yanayokatalika akilini na katika dhamiri za wanadamu. Hivyo sharti ya kwanza ya Kitabu cha Mungu ni kwamba, kama vile mti mzuri wa matunda, wenye mizizi imara iliyoshika ardhini, Kitabu hicho kiwe na misingi imara, kiendelee kupata uhai mpya kule kilikotoka, kitosheleze haja za watu, na uketo na upana wa maana ya maneno yake usiwe na kikomo.

(2) Kama vile mti imara wenye mizizi iliyozama ardhini, Kitabu hicho kikae vile vile kilivyo na kisihemewe na mabadiliko yanayotokea katika maoni na hali za watu; wala kisishindwe na upinzani unaoletwa na watu, na mtu anayekifuata kwa kutenda mafundisho kinayoyaeleza aridhike nacho kabisa.

(3) Kama vile mti imara wenye matawi yanayofika angani, Kitabu hicho kiwe na maisha marefu na kisibadilike au kutanguka, na kiwe kizuri na chema katika kila hali.

(4) Na kama vile mti mwema hutoa matunda yake kwa wingi na kila msimu, Kitabu hicho kiendelee kuwa na kundi la wafuasi ambao kwa kufuata mafundisho yake wawe mfano wa tabia zilizo bora na nzuri zinazofundishwa na Kitabu hicho, na kiwe chenye kuridhisha kabisa.

(5) Kama vile mti mwema unavyotoa matunda kwa idhini ya Mola wake, Kitabu hicho kipate uhai na nguvu kutoka kwa Allah na hivyo kisiwe na maneno ya kigeugeu na mafundisho yake yawe yanayopatana, nacho kivishinde Vitabu vingine vyote vilivyoshuka, katika sifa hizi.

Katika vitabu vyote vya dini utaona ya kwamba Qur'an tu ndiyo yenye sifa zote hizo kwa kipimo kilicho kamili. Kwa lugha tamu kabisa na nyepesi imeeleza habari zote ngumu ngumu zinazohusu mambo ya tabia na ya kiroho ya mwanadamu. Qur'an imetosheleza na itaendelea kutosheleza haja zote za namna mbalimbali za wanadamu. Kanuni zake na mafundisho yake yanafuatika na yanatendeka katika nyakati zote. Katika zama zote zilizopita imetoa watu ambao, kwa kuifuata, wakaweza kujiunganisha na Allah, na Allah akazungumza nao sana. Watu wa namna hii wataendelea kutokea katika wafuasi wa Qur'an. Qur'an kila inapojaribiwa haikutwi imepunguka. Mti wa Qur'an hautanyauka wala kuoza na utaendelea kutoa matunda mazuri mpaka mwisho wa dahari.

27. Na mfano wa neno baya ni kama mti mbaya ambao umeng'olewa ardhini, hauna uimara.

وَمَثَلُ كَلِمَةٍ خَبِيْثَةٍ كَشَجَرَةٍ خَبِيْثَةِ ِۨ اجْتُثَّتْ مِنْ فَوْقِ الْاَرْضِ مَا لَهَا مِنْ قَرَارٍ ﴿٢٧﴾

28. Allah Huwaimarisha wale walioamini kwa kauli thabiti, katika maisha ya dunia na katika Akhera; na Allah Huwaangamiza wadhalimu. Na Allah Hufanya Apendavyo.

يُثَبِّتُ اللّٰهُ الَّذِيْنَ اٰمَنُوْا بِالْقَوْلِ الثَّابِتِ فِى الْحَيٰوةِ الدُّنْيَا وَفِى الْاٰخِرَةِ ۚ وَيُضِلُّ اللّٰهُ الظّٰلِمِيْنَ ۙ وَيَفْعَلُ اللّٰهُ مَا يَشَآءُ ﴿٢٨﴾ ع ١٤

FUNGU 5

29. Je, hukuwaona wale waliobadilisha neema ya Allah kwa kufuru na kuwafikisha watu wao kwenye nyumba ya maangamio-

اَلَمْ تَرَ اِلَى الَّذِيْنَ بَدَّلُوْا نِعْمَتَ اللّٰهِ كُفْرًا وَّاَحَلُّوْا قَوْمَهُمْ دَارَ الْبَوَارِ ﴿٢٩﴾

30. (Ambayo ni) Jahanamu. Wataiingia; na ni mahali pabaya pa kukaa.

جَهَنَّمَ ۚ يَصْلَوْنَهَا ؕ وَبِئْسَ الْقَرَارُ ﴿٣٠﴾

31. Na wakamfanyia Allah washirika ili kupoteza (watu) katika njia Yake. Sema: Jifurahisheni kidogo, kisha hakika marudio yenu ni kwenye Moto.

وَجَعَلُوْا لِلّٰهِ اَنْدَادًا لِّيُضِلُّوْا عَنْ سَبِيْلِهٖ ؕ قُلْ تَمَتَّعُوْا فَاِنَّ مَصِيْرَكُمْ اِلَى النَّارِ ﴿٣١﴾

32. Waambie watumishi wangu walioamini, wasimamishe Sala, na watoe katika vile Tulivyowaruzuku, kwa siri na dhahiri, kabla haijafika siku isiyo na biashara wala urafiki.

قُلْ لِّعِبَادِىَ الَّذِيْنَ اٰمَنُوْا يُقِيْمُوا الصَّلٰوةَ وَيُنْفِقُوْا مِمَّا رَزَقْنٰهُمْ سِرًّا وَّعَلَانِيَةً مِّنْ قَبْلِ اَنْ يَّاْتِىَ يَوْمٌ لَّا بَيْعٌ فِيْهِ وَلَا خِلٰلٌ ﴿٣٢﴾

Aya 27. Kitabu cha dini kinachobuniwa na wanadamu kimefanana na mti mbaya, hakidumu, mafundisho yake hayakubaliwi na akili wala hayakubaliwi na kanuni za asili, hakimudu upinzani na mafundisho yake yanabadilika-badilika kama zinavyobadilika hali za watu. Kinakuwa na mchanganyiko wa mafundisho ya kushuku-shuku. Kinashindwa kuwatoa watu wanaoweza kudai kuwa wamefungamana na Allah kwa kweli, na hakipati misaada mipya kutoka kwa Allah. Hii ndiyo hali ya vitabu vilivyotungwa na Manabii wa uwongo; au Vitabu vilivyotoka kwa Mungu lakini kwa kuwa havikukusudiwa kudumu milele, mara vilipomaliza kazi vilivyokusudiwa, havikulindwa na Allah, na vikaachwa na kujiharibikia, na watu wakaingiza ndani yao maneno na kutoa mengine kama walivyopenda.

Aya 29. *Neema ya Allah* hapa ni wahyi ambao unasemwa katika Aya iliyotangulia kuwa "kauli thabiti." Allah aliwapa wanadamu neema hii, lakini badala ya kutoa shukurani wao wakakufuru, na pia wakajiangamiza kwa kuukataa.

اَللّٰهُ الَّذِیْ خَلَقَ السَّمٰوٰتِ وَالْاَرْضَ
وَاَنْزَلَ مِنَ السَّمَآءِ مَآءً فَاَخْرَجَ بِهٖ مِنَ
الثَّمَرٰتِ رِزْقًا لَّكُمْ ۚ وَسَخَّرَ لَكُمُ
الْفُلْكَ لِتَجْرِیَ فِی الْبَحْرِ بِاَمْرِهٖ ۚ
وَسَخَّرَ لَكُمُ الْاَنْهٰرَ ﴿۳۳﴾

33. Allah ndiye Aliyeziumba mbingu na ardhi na Akateremsha maji kutoka mawinguni, na kwayo akaotesha matunda kuwa riziki kwa ajili yenu, na Akawatiishieni merikebu ili zipite katika bahari kwa amri Yake, na Akawatiishieni mito.

وَسَخَّرَ لَكُمُ الشَّمْسَ وَالْقَمَرَ
دَآئِبَیْنِ ۚ وَسَخَّرَ لَكُمُ الَّیْلَ وَالنَّهَارَ ﴿۳۴﴾

34. Na Akawatiishieni jua na mwezi, vifanyavyo kazi mfululizo. Na Akawatiishieni usiku na machana.

وَاٰتٰىكُمْ مِّنْ كُلِّ مَا سَاَلْتُمُوْهُ ؕ
وَاِنْ تَعُدُّوْا نِعْمَتَ اللّٰهِ لَا تُحْصُوْهَا ؕ
اِنَّ الْاِنْسَانَ لَظَلُوْمٌ كَفَّارٌ ﴿۳۵﴾ ع ۴

35. Na Amewapeni kila mlichomwomba; na kama mkihesabu neema za Allah, hamtaweza kuzihesabu. Bila shaka mwanadamu ni mdhalimu mkubwa, asiye shukurani.

FUNGU 6

وَاِذْ قَالَ اِبْرٰهِیْمُ رَبِّ اجْعَلْ هٰذَا الْبَلَدَ
اٰمِنًا وَّاجْنُبْنِیْ وَبَنِیَّ اَنْ نَّعْبُدَ
الْاَصْنَامَ ﴿۳۶﴾ ؕ

36. Na (kumbuka) aliposema Ibrahimu: Mola wangu, Ujaalie mji huu uwe wa amani, na Ukanitenge mimi na wanangu tusiabudu masanamu.

رَبِّ اِنَّهُنَّ اَضْلَلْنَ كَثِیْرًا مِّنَ النَّاسِ ۚ
فَمَنْ تَبِعَنِیْ فَاِنَّهٗ مِنِّیْ ۚ وَمَنْ عَصَانِیْ
فَاِنَّكَ غَفُوْرٌ رَّحِیْمٌ ﴿۳۷﴾

37. Mola wangu, hakika (waungu) hawa wamewapoteza wengi katika watu. Basi aliyenifuata yu katika mimi; na aliyeniasi, basi Wewe hakika ni Msamehevu, Mrehemevu.

Aya 33 na **34.** Katika Aya hizi, Qur'an imehesabu baadhi ya fadhili za Allah. Sababu ya kufanya hivyo ni kuwa, kwanza kuonyesha ya kwamba vitu vyote vimeumbwa ili mwanadamu avitumie. Lakini mwanadamu akifanya upumbavu wa kuviabudu badala ya kuvifanyia matumizi vilivyoumbiwa, basi atavinyimwa. Pili, kwa kuwa fadhili hizi zinatoka kwa Allah, basi watazipewa wale wanaofuata maagizo ya Allah na kuishi maisha ya ucha-Mungu. Hivyo ndivyo ilivyotokea, na ulimwengu mzima ulisimama wima kama mtumishi ili kuusaidia Uislamu.

Aya hii pia inawaonya Waislamu ya kwamba fadhili wanazopewa na Mungu wasifikiri ni kwa ajili yao tu, bali wawafaidishe nazo viumbe wenzao, kwa maana vitu vilivyoumbwa na Allah vimekusudiwa kwa ajili yetu sisi sote, na viumbe wote wa Allah wana haki navyo, wala siyo vifaidiwe na watu maalumu au kabila maalumu tu.

38. Mola wetu, hakika mimi nimewakalisha baadhi ya wazao wangu katika bonde lisilozaa karibu na Nyumba Yako Takatifu - Mola wetu, - ili wasimamishe Sala. Basi Ujaalie mioyo ya watu ielekee kwao na Uwaruzuku matunda ili wapate kushukuru.

رَبَّنَآ اِنِّيْٓ اَسْكَنْتُ مِنْ ذُرِّيَّتِيْ بِوَادٍ غَيْرِ
ذِيْ زَرْعٍ عِنْدَ بَيْتِكَ الْمُحَرَّمِ ۙ رَبَّنَا
لِيُقِيْمُوا الصَّلٰوةَ فَاجْعَلْ اَفْئِدَةً مِّنَ
النَّاسِ تَهْوِيْٓ اِلَيْهِمْ وَارْزُقْهُمْ
مِّنَ الثَّمَرٰتِ لَعَلَّهُمْ يَشْكُرُوْنَ ﴿٣٨﴾

39. Mola wetu, hakika Wewe Unajua tunayoyaficha na tunayoyadhihirisha. Na hakuna cho chote kinachofichika kwa Allah katika ardhi wala katika mbingu.

رَبَّنَآ اِنَّكَ تَعْلَمُ مَا نُخْفِيْ وَمَا نُعْلِنُ ؕ
وَمَا يَخْفٰى عَلَى اللّٰهِ مِنْ شَيْءٍ فِي الْاَرْضِ
وَلَا فِي السَّمَآءِ ﴿٣٩﴾

40. Sifa zote njema zinamhusu Allah Aliyenipa, juu ya uzee (wangu), Ismaili na Isihaka. Hakika Mola wangu ni Asikiaye sana maombi.

اَلْحَمْدُ لِلّٰهِ الَّذِيْ وَهَبَ لِيْ عَلَى الْكِبَرِ
اِسْمٰعِيْلَ وَ اِسْحٰقَ ؕ اِنَّ رَبِّيْ
لَسَمِيْعُ الدُّعَآءِ ﴿٤٠﴾

41. Mola wangu, Unijaalie niwe msimamisha Sala, na wazao wangu (pia); Mola wetu, na Upokee maombi yangu.

رَبِّ اجْعَلْنِيْ مُقِيْمَ الصَّلٰوةِ وَمِنْ
ذُرِّيَّتِيْ ۖ رَبَّنَا وَتَقَبَّلْ دُعَآءِ ﴿٤١﴾

Aya 38. Aya hii inaeleza matokeo ya njozi aliyoona Nabii Ibrahimu ya kwamba anamchinja mwanawe Ismaili (sura 37:103). Kwa kuwa zamani zile desturi ya kuwachinja watu kama kafara ilikuwa imeenea sana, Nabii Ibrahimu akamchukua mwanawe kwenda mchinja. Lakini mradi wa ndoto ile ulikuwa ya kwamba atamweka mwanawe katika bonde lisilozaa cho chote; maana kumwacha kijana mdogo mahali pasipokuwa maji wala mimea wala alama yo yote ya uhai ni sawa na kumchinja kama kafara. Lakini Nabii Ibrahimu kutimiza ndoto yake kikwelikweli kulileta tukio moja lenye nguvu. Alipomlaza Ismaili na kisu kiko juu ya koo lake, tayari kumchinja, akakatazwa na Allah, na toka hapo desturi ya kuwachinja wanadamu kama kafara ikakomeshwa kwa wafuasi wa Mungu.

Aya 40. *Ismaa'iil* (Ismaili) ni jina ambalo maana yake ni "Mungu alisikia dua." Ismaili alikuwa mtoto mkubwa wa Nabii Ibrahimu aliyezaliwa na mkewe wa Kimisri, Hajira. Nabii Ibrahimu alipokuwa na umri wa miaka themanini na sita alimzaa Ismaili baada ya kumwomba Mungu ampe mtoto. Nabii Ismaili alizaa watoto kumi na mbili, maarufu kati ya watoto hao ni Kedar, babu mkuu wa taifa la Waarabu (Enc. Bib. & Jew. Enc.). Pia tazama sura 2:128-130.

Is'haaq (Isihaka) alikuwa mtoto wa pili wa Nabii Ibrahimu aliyezaliwa na mkewe, Sarah. Isihaka ndiye aliyemzaa Yakubu anayeitwa Israeli, ambaye ni Baba mkuu wa Taifa la Waisraeli. Isihaka ndiye anafikiriwa na Wakristo na Mayahudi kwamba alitolewa kuchinjwa na Nabii Ibrahimu kwa kutaka kutimiza ndoto yake. Lakini ushahidi wa historia na wa Biblia unapinza hiyo fikira yao.

42. Mola wetu, Unighofirie mimi na wazazi wangu na waaminio siku ya kusimama hesabu.

رَبَّنَا اغْفِرْ لِيْ وَلِوَالِدَيَّ وَلِلْمُؤْمِنِيْنَ يَوْمَ يَقُوْمُ الْحِسَابُ ﴿٤٢﴾ ع ١٨

FUNGU 7

43. Wala usidhani Allah Ameghafilika na wanayoyafanya wadhalimu. Hakika Yeye Anawapa muhula mpaka siku ambayo macho (yao) yatakodoa bila kukapua.

وَلَا تَحْسَبَنَّ اللّٰهَ غَافِلًا عَمَّا يَعْمَلُ الظّٰلِمُوْنَ ۬ؕ اِنَّمَا يُؤَخِّرُهُمْ لِيَوْمٍ تَشْخَصُ فِيْهِ الْاَبْصَارُ ﴿٤٣﴾ۙ

44. Wakiharakia kwa hofu, wakiinua vichwa vyao, na macho yao hayatawarudia, na mioyo yao itakuwa mitupu.

مُهْطِعِيْنَ مُقْنِعِيْ رُءُوْسِهِمْ لَا يَرْتَدُّ اِلَيْهِمْ طَرْفُهُمْ ۚ وَاَفْـِٕدَتُهُمْ هَوَآءٌ ﴿٤٤﴾

45. Na uwaonye watu siku ambayo itawafikia adhabu, ndipo waliodhulumu watasema: Mola wetu, Utuahirishe mpaka muda ulio karibu. Tutaitikia wito Wako na tutawafuata Mitume. Je, hamkuwa mmeapa zamani ya kwamba ninyi hamtapata maanguko?

وَاَنْذِرِ النَّاسَ يَوْمَ يَاْتِيْهِمُ الْعَذَابُ فَيَقُوْلُ الَّذِيْنَ ظَلَمُوْا رَبَّنَاۤ اَخِّرْنَاۤ اِلٰۤى اَجَلٍ قَرِيْبٍ ۙ نُّجِبْ دَعْوَتَكَ وَنَتَّبِعِ الرُّسُلَ ؕ اَوَلَمْ تَكُوْنُوْۤا اَقْسَمْتُمْ مِّنْ قَبْلُ مَا لَكُمْ مِّنْ زَوَالٍ ﴿٤٥﴾ۙ

46. Hali mmekaa katika makao ya wale waliodhulumu nafsi zao, na imewadhirikieni jinsi Tulivyowafanya: na Tumewaelezeni methali (zote).

وَّسَكَنْتُمْ فِيْ مَسٰكِنِ الَّذِيْنَ ظَلَمُوْۤا اَنْفُسَهُمْ وَتَبَيَّنَ لَكُمْ كَيْفَ فَعَلْنَا بِهِمْ وَضَرَبْنَا لَكُمُ الْاَمْثَالَ ﴿٤٦﴾

Aya 42. *Ighfirlii*, "Unighofirie." Dua hii huwa na maana nyingine inaposemwa na Manabii wa Mungu iliyo tofauti na ile inayotoa endapo mtu mwenye dhambi ndiye anayeiomba. Mtume wa Mungu anapoomba *ghufraan* au *maghfira* (samahani) neno hilo maana yake linakuwa kumfunika kwa rehema Yake na kumlinda na matokeo yenye dhara ya udhaifu wa kibinadamu.

Lakini kama mtu mwenye dhambi anaomba kwa Allah kwa maneno *Allahummaghfirlii* (Mola wangu, nighofirie), kwa hakika anamwomba amlinde na matokeo mabaya ya dhambi zake, na amlinde na adhabu ambayo imewekwa kwa ajili ya dhambi hiyo; na pia amlinde asifanye dhambi nyingine.

Ni desturi ya maneno ya Kiarabu ya kwamba maneno yake yana namna nyingi mbalimbali za maana, na mara kwa mara neno moja linakuwa na maana mbalimbali katika matokeo mbalimbali, na neno *ghafr* ni moja la namna hii. Kwa mfano *neno Jabaar*, linapotumiwa kwa ajili ya Allah, maana yake inakuwa "Anayekirejesha kitu kwenye hali iliyo njema"; lakini linapotumiwa kwa mwanadamu, maana yake inakuwa "mtu anayepita kiasi katika maasi na uovu."

47. Na walifanya kila aina ya hila waliyoweza, lakini matokeo ya hila zao yako mikononi mwa Allah, hata kama hila zao ziwe na uwezo wa kusogeza milima.

وَقَدْ مَكَرُوْا مَكْرَهُمْ وَعِنْدَ اللّٰهِ مَكْرُهُمْ ؕ وَاِنْ كَانَ مَكْرُهُمْ لِتَزُوْلَ مِنْهُ الْجِبَالُ ﴿٤٦﴾

48. Basi usimdhanie Allah ni Avunjaye ahadi Yake kwa Mitume Wake. Bila shaka Allah ni Mshindi, Mwenye kuadhibu.

فَلَا تَحْسَبَنَّ اللّٰهَ مُخْلِفَ وَعْدِهٖ رُسُلَهٗ ؕ اِنَّ اللّٰهَ عَزِيْزٌ ذُو انْتِقَامٍ ﴿٤٧﴾

49. Siku ardhi itabadilishwa kuwa ardhi nyingine, na mbingu (pia); nao watahudhuria mbele ya Allah, Mmoja, Mwenye nguvu.

يَوْمَ تُبَدَّلُ الْاَرْضُ غَيْرَ الْاَرْضِ وَالسَّمٰوٰتُ وَبَرَزُوْا لِلّٰهِ الْوَاحِدِ الْقَهَّارِ ﴿٤٨﴾

50. Na utawaona wakosefu siku hiyo wamefungwa katika minyororo.

وَتَرَى الْمُجْرِمِيْنَ يَوْمَئِذٍ مُّقَرَّنِيْنَ فِي الْاَصْفَادِ ﴿٤٩﴾

51. Kanzu zao zitakuwa za lami, na Moto utazifunika nyuso zao.

سَرَابِيْلُهُمْ مِّنْ قَطِرَانٍ وَّتَغْشٰى وُجُوْهَهُمُ النَّارُ ﴿٥٠﴾

52. Ili Allah Ailipe kila nafsi yale iliyoyachuma. Hakika Allah ni Mwepesi wa kuhesabu.

لِيَجْزِيَ اللّٰهُ كُلَّ نَفْسٍ مَّا كَسَبَتْ ؕ اِنَّ اللّٰهَ سَرِيْعُ الْحِسَابِ ﴿٥١﴾

53. Huu ni ujumbe uliotolewa wazi-wazi kwa faida ya binadamu ili wapate kuonywa kwa huo na ili wajue kwamba Yeye ni Mungu Mmoja wa pekee na ili kwamba wale wenye akili waweze kushika nasaha.

هٰذَا بَلٰغٌ لِّلنَّاسِ وَلِيُنْذَرُوْا بِهٖ وَلِيَعْلَمُوْٓا اَنَّمَا هُوَ اِلٰهٌ وَّاحِدٌ وَّلِيَذَّكَّرَ اُولُوا الْاَلْبَابِ ﴿٥٢﴾ ع ١٤

Aya 49. Aya hii inaeleza habari ya siku ya Kiyama, zitakapoletwa mbingu mpya na ardhi mpya. Inaonekana ya kwamba neema za Akhera zitakuwa tofauti na hizi za dunia hii, maana Aya inasema, ardhi hii na mbingu hii vitabadilishwa kwa ardhi nyingine na mbingu nyingine. Kama ardhi hii hii na mbingu hii hii ndivyo vitaumbwa tena katika Akhera, pamoja na matunda haya haya na vifaa hivi hivi tunavyovitumia hapa duniani, patakuwa na haja gani kubadilisha ardhi na mbingu za zamani?

Aya 53. *Haya yatosha kuwa mauidha kwa watu*, yaani ukweli umekwisha fikishwa sawasawa kwa watu kwa njia ya Kitabu hiki, na sasa ni shauri yao kukubali au kukataa.

سُوْرَةُ الْحِجْرِ مَكِّيَّةٌ وَّ هِيَ مَعَ الْبَسْمَلَةِ مِائَةُ اٰيَةٍ وَّ سِتَّةُ رُكُوْعَاتٍ

15. SURA AL-HIJR

Imeteremshwa Makka

Ina mafungu 6 na Aya 100 pamoja na Bismillahi

بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ ①

1. Kwa jina la Allah, Mwingi wa rehema, Mwingi wa ukarimu.

الٓرٰ ۟ تِلْكَ اٰيٰتُ الْكِتٰبِ وَقُرْاٰنٍ مُّبِيْنٍ ②

2. Mimi ni Allah Nionaye. Hizi ni Aya za Kitabu na za Qur'an ielezayo.

Maoni ya wanazuoni ni kwamba Sura hii yote ilishuka Makka. Abu Hayyan anasema ya kuwa sura hii ni ya Makka na wanazuoni wote hawahitilafiani juu ya jambo hili (Muhit). Mambo yanayoelezwa katika sura hii yanapata nguvu zaidi kwa vile pia sura hii imeshuka Makka.

Habari za neno *Hijr* ambalo ni jina la Sura hii zimeelezwa katika Aya 81.

Aya 2. *Alif Laam Raa,* "Mimi ndiye Allah Nionaye." Tazama sura 2:2.

Aya za Kitabu na za Qur'an. Hapa neno la Mungu limeitwa *Kitaab,* yaani kilichoandikwa; na pia limeitwa *Qur'aan*, yaani kinachosomwa; ili kuonyehsa ya kuwa neno hili litahifadhiwa kwa kuandikwa na kwa kusomwa. Hivi ndivyo hasa ilivyokuwa, maana katika vitabu vyote vilivyoshuka, ni Aya za Qur'an tu zilizoandikwa mara baada ya kushuka; na kadhalika zikahifadhiwa moyoni na maelfu kwa maelfu ya Waislamu katika karne 14 zilizopita. Desturi ya kuhifadhi Qur'an moyoni ilianza toka siku za Mtume s.a.w. na katika kila zama kumekuwako maelfu ya Waislamu wanaoweza kuisoma Qur'an yote kwa moyo. Hii ni heshima ambayo hakuna Kitabu kingine cho chote cha dini kilicho nayo. Hata kama nakala zote za Qur'an zipotee, Qur'an haitatoweka hapa duniani, maana imeandikwa kwa namna isiyofutika katika nyoyo za watu maelfu kwa maelfu, toka mwanzo wa dunia mpaka mwisho. Hivyo ahadi ya Allah iliyoelezwa katika Aya ya 10 ya sura hii ikatimia kwa namna ya ajabu.

Hapa pana jambo moja linalotakiwa kutazamwa vizuri. Ni mahali pawili tu katika Qur'an nzima neno Qur'an na Kitabu yametumiwa pamoja, napo ni katika sura 27:2 na hapa. Katika Aya hii neno Kitabu limewekwa kabla ya neno Qur'an, hali katika sura 27:2 neno Qur'an ndilo limewekwa kabla ya neno Kitabu. Kama ilivyoelezwa juu, neno Kitabu linaashiria ya kwamba Kitabu hiki kitukufu kitaendelea kuandikwa, na neno Qur'an linaashiria ya kwamba Kitabu hiki kitakuwa kinasomwa mara kwa mara na kwa wingi sana. Sasa katika Aya hii neno mubiin (ielezayo) limekuwa ni sifa ya neno Qur'an, katika sura 27:2 neno hilo limekuwa ni sifa ya neno Kitabu. Jambo hili linaonyesha ya kwamba habari iliyomo katika sura hii inashughulika zaidi na sifa iliyotiwa juu ya Qur'an kuliko iliyotiwa juu ya Kitabu. Lakini katika sura 27:2 mpango umefanywa kinyume cha huu kwa sababu nguvu kubwa inatiwa juu ya mabadiliko yatakayoletwa na Qur'an katika hali ya kuwa i *Kitaab* (yaani Kitabu kilichoandikwa).

Katika sura hii habari za maisha ya Manabii (kama Adamu, Ibrahimu, Luti na Saleh) zimeelezwa ambao katika nyakati zao haukuwako ufundi wa kuandika au haukujulikana sana, na elimu ilikuwa ya maelezo ya mdomo tu; ambapo katika sura 27 zimeelezwa habari za maisha ya Manabii (kama Musa na Daudi) ambao katika nyakati zao kuandika kulikuwa kumeenea, na elimu ikawa ya kuandika si ya kuhifadhi moyoni kama ilivyokuwa zamani.

JUZU 14

3. Mara nyingi wale waliokufuru wanapenda laiti wangalikuwa Waislamu.

رُبَمَا يَوَدُّ الَّذِيْنَ كَفَرُوْا لَوْ كَانُوْا مُسْلِمِيْنَ ۝٢

4. Waache wale (chakula) na wanufaike kwa muda na liwadanganye tumaini la uwongo; kwani hivi karibuni watajua.

ذَرْهُمْ يَاْكُلُوْا وَيَتَمَتَّعُوْا وَيُلْهِهِمُ الْاَمَلُ فَسَوْفَ يَعْلَمُوْنَ ۝٣

5. Na Hatukuuangamiza mji wo wote ila ulikuwa na hukumu maalumu.

وَمَآ اَهْلَكْنَا مِنْ قَرْيَةٍ اِلَّا وَلَهَا كِتَابٌ مَّعْلُوْمٌ ۝٤

6. Hawawezi watu wo wote kuitangulia ajali yao, wala hawawezi kuikawiza.

مَا تَسْبِقُ مِنْ اُمَّةٍ اَجَلَهَا وَمَا يَسْتَاْخِرُوْنَ ۝٥

7. Na wakasema: Ewe uliyeteremshiwa mawaidha, hakika wewe ni mwehu.

وَقَالُوْا يٰٓاَيُّهَا الَّذِيْ نُزِّلَ عَلَيْهِ الذِّكْرُ اِنَّكَ لَمَجْنُوْنٌ ۝٦

8. Mbona hutuletei Malaika ikiwa wewe u miongoni mwa wasemao kweli?

لَوْ مَا تَاْتِيْنَا بِالْمَلٰٓئِكَةِ اِنْ كُنْتَ مِنَ الصّٰدِقِيْنَ ۝٧

9. Sisi Hatuteremshi Malaika ila kwa haki, na hapo hawatapewa muda.

مَا نُنَزِّلُ الْمَلٰٓئِكَةَ اِلَّا بِالْحَقِّ وَمَا كَانُوْٓا اِذًا مُّنْظَرِيْنَ ۝٨

10. Hakika Sisi Tumeyateremsha mawaidha haya na hakika Sisi ndio Tuyalindao.

اِنَّا نَحْنُ نَزَّلْنَا الذِّكْرَ وَاِنَّا لَهٗ لَحٰفِظُوْنَ ۝٩

Pia inafaa kuangalia ya kwamba ambapo maneno *Qur'aanum-mubiin* (Qur'an ielezayo) yametumiwa katika Qur'an mara mbili tu, maneno *Kitaabum-mubiin* (Kitabu kielezacho) yametumiwa mara zisizopungua kumi na mbili. Hii ni kutaka kudokeza ya kwamba taarifa iliyoandikwa ni yenye faida zaidi kuliko taarifa wanayopokezana watu mdomo kwa mdomo. Kwa hiyo Waislamu ni lazima washughulike zaidi na kupata elimu na kusoma elimu iliyoandikwa.

Aya 3. Hata hivi leo wako ambao si Waislamu wanaotamani wangekuwa Waislamu. Kwa mfano, Wakristo walipolazimika kutoa sheria ya kuruhusu talaka hata kwa kosa lisilo la zinaa, bila shaka walitamani laiti dini yao ingekuwa na mafundisho kama ya Kiislamu.

Aya 5. *Hukumu maalumu,* hapa mradi wake ni wakati uliowekwa kwa ajili ya kuwahilikisha maadui wa Mtume, na ni wakati ambao ulitabiriwa naye. Maadui wa Mtume hawafikiwi na adhabu ila iliyobashiriwa.

Aya 10. Ahadi ya kuihifadhi Qur'an imetimia barabara, na hata kama kusiwe na dalili nyingine, hii tu inatosha kuhakikisha kuwa Kitabu hiki kimetoka kwa Allah. Kutobadilika kwa Qur'an toka imeteremshwa kwa Mtume s.a.w. ni jambo linalokubaliwa hata na waipinzao dini ya Kiislamu, kama Sir William Muir (Introduction to the Life of Muhammad). Professor Noldeke, mwanachuoni mustashriki (orientalist) mkuu wa Kijerumani pia anakubali jambo hili (Enc. Brit.). Kadhalika Professor Nicholson anakubali kuhifadhika Qur'an (Literary History of the Arabs).

(1) Sir William Muir amesema, Dalili hizi zote zinaleta utulivu moyoni ya kuwa Qur'an tunayosoma ni neno kwa neno ile ile Muhammad aliyowasomea watu" (The Koran ukurasa 40).

(2) Tena yeye huyo amesema, "Hakuna shaka katika jambo hili ya kuwa Qur'an hii ni ile ile aliyotutolea Muhammad." (Life of Muhammad).

(3) Professor Noldeke amesema, "Qur'an aliyoweka Uthman mbele ya dunia ilikuwa ni ile ile aliyotoa Muhammad, ingawa taratibu yake ni ya ajabu. Juhudi ya wanazuoni wa Ulaya kuhakikisha ya kuwa yaliingia mabadiliko katika Qur'an imeshindwa" (Encyclopaedia Britannica, chini ya neno "Qur'an").

Ukilinganisha Biblia na Qur'an katika jambo hili, utaona wazi ya kuwa Biblia kimekuwa kitabu cha kibinadamu, kisicho sahihi, na kilichojaa makosa. Hartzel Spence ameandika ya kuwa katika mwaka 1720 wanazuoni wa Kiingereza walikadiria kuwamo makosa 20,000 (ishirini elfu) katika Agano Jipya linalosomwa na Waprotestanti na Wakatoliki, na wanazuoni wa sasa wanakadiria makosa hayo kuwa 50,000, ambayo yamewafanya wanazuoni wakubwa-wakubwa wa Kikristo 125 wakutanishe vichwa kukagua vitabu vyao na kuona maneno gani ni ya asili, na yepi yameingizwa baadaye. (Review of Religions, August, 1952).

Katika East African Standard ya tarehe 23 December, 1952, imetolewa taarifa ya kwamba leo hii ziko muswada 4,500 za Biblia ambazo zilikuwa hazijapatikana wakati iliposahihishwa Biblia katikati ya miaka ya 1870 na 1885. Hivyo sasa wameweza kusahihisha "mengi katika makosa" yaliyokuwa katika Biblia za zamani. Kumbukeni ya kwamba makosa yote hayo yalikuwa yanaitwa "Neno la Mungu," na yanaitwa hivyo mpaka kesho.

Kazi ya kutengeneza Biblia mpya inayoitwa *Revised Standard Version* imefanywa huko Amerika na wanazuoni wa Kikristo wa *International Council of Religious Education* wa madhehebu 40 za Wakristo. Hata hivyo hawakuweza kupata muswada ambayo ni ya asili; asemavyo Hartzel Spence, "Hakuna maandiko ya asili ya Biblia, au hata ya Agano Jipya, yanayoonekana. Kwa hakika hakuna hata ukurasa mmoja wa maandiko ya asili. Lakini kuna muswada nyingi za tarehe toka miaka 200 baada ya Kristo ambazo zilinakiliwa toka maandiko yaliyozitangulia." (Review of Religions, August, 1952).

Biblia hiyo mpya ya Kiingereza imeondolewa makosa mengine ambayo hayajaondolewa katika Biblia mpya ya Kiswahili iitwayo *Revised Version.* Ile Biblia iitwayo *Authorised Version* ya wakati wa King James sasa imekuwa si sahihi hali kwanza iliitwa Biblia Takatifu. Katika hii tafsiri mpya, mahali palipoandikwa "mwanamume" wanawake wa Amerika wamedai neno hilo lifutwe na badala yake liandikwe neno "mtu" ili liwahusu na wanawake pia. Neno la Mungu kufutwa na kubadilishwa kwa ajili ya malalamiko ya wanawake ni kisa cha ajabu cha vitabu vya hawa jamaa zetu. Isitoshe, katika Kitabu cha Isaya 7:14 panaposema, "Tazama, bikira atachukua mimba, atazaa mtoto mwanamume," sasa neno "bikira" wamelifuta kwamba ni kosa, na badala yake wameandika "mwanamke kijana." Kadhalika kifungu cha mwisho cha Mathayo 6:13 kisemacho, "Kwa kuwa ufalme ni wako, na nguvu na utukufu, hata milele. Amina" kadhalika kimefutwa kuwa ni kosa. Je, Kitabu cha namna hii kinaweza kuwa cha Mungu? Mapadre watasemaje sasa baada ya siri kufichuka?

Toka mwanzo Qur'an ilitangaza kazi hii ya Wakristo kuandika vitabu kwa mikono yao na kusema ni neno limetoka kwa Mungu, na imewaonya sana na kuwahadharisha na adhabu kali kwa jambo hili (tazama sura 2:80). Na kadhalika Qur'an ilituahidi kuwa tutaendelea kuona hiyana za watu hawa (sura 5:14).

Ingawa sasa mtindo umekuwa kuwakazania Waafrika wasome Biblia, lakini huko Uingereza watu wamekwisha choka nayo. Imeandikwa, "Nyumba nyingi za Waingereza hazina Biblia, na katika nyumba nyingine Biblia inatumiwa kwa kufumbua mafumbo ya maneno, anasema Askofu Mkuu wa York, Dr. Cyril Garbett. Dr. Garbett aliwaambia wanachama wa British and Foreign Bible Society waliohudhuria mkutano wa mwaka katika London ya kwamba Waingereza wengi hawasomi Biblia asilan, nao hawana hata nia ya kusoma" (Reuter: *East African Standard*, 9th May, 1952). Nasi tunafikiri wakati wa Waafrika kuiachilia mbali Biblia unasogea upesi upesi maadamu elimu yao inazidi.

Lakini Qur'an Takatifu ni Kitabu kilichohifadhiwa kabisa, kisicho mageuzi, mazidisho wala mapunguzi, kama wanavyokiri hata maadui wa Uislamu. Na ahadi ya Allah ya kuwa Qur'an italindwa imethibitika.

وَلَقَدْ اَرْسَلْنَا مِنْ قَبْلِكَ فِيْ شِيَعِ الْاَوَّلِيْنَ ﴿١١﴾

11. Na bila shaka Tulikwisha watuma (Mitume) kabla yako katika makundi ya (watu) wa kwanza.

وَمَا يَاْتِيْهِمْ مِّنْ رَّسُوْلٍ اِلَّا كَانُوْا بِهٖ يَسْتَهْزِءُوْنَ ﴿١٢﴾

12. Na hakuwafikia Mtume ye yote isipokuwa walimfanyia mzaha.

كَذٰلِكَ نَسْلُكُهٗ فِيْ قُلُوْبِ الْمُجْرِمِيْنَ ﴿١٣﴾

13. Hivi ndivyo Tunavyoiingiza (tabia ya mzaha) katika mioyo ya wakosefu.

لَا يُؤْمِنُوْنَ بِهٖ وَقَدْ خَلَتْ سُنَّةُ الْاَوَّلِيْنَ ﴿١٤﴾

14. Hawayaamini hali umekwisha pita mfano wa watu wa kwanza.

وَلَوْ فَتَحْنَا عَلَيْهِمْ بَابًا مِّنَ السَّمَآءِ فَظَلُّوْا فِيْهِ يَعْرُجُوْنَ ﴿١٥﴾

15. Na lau Tungaliwafungulia mlango wa mbingu, na wakaanza kupanda humo,

لَقَالُوْٓا اِنَّمَا سُكِّرَتْ اَبْصَارُنَا بَلْ نَحْنُ قَوْمٌ مَّسْحُوْرُوْنَ ﴿١٦﴾

16. Hakika wangalisema: Macho yetu yameleweshwa tu, bali sisi ni watu tuliologwa.

FUNGU 2

وَلَقَدْ جَعَلْنَا فِي السَّمَآءِ بُرُوْجًا وَّزَيَّنّٰهَا لِلنّٰظِرِيْنَ ﴿١٧﴾

17. Na hakika Tumeweka katika mbingu vituo vya nyota na kuipamba kwa ajili ya watazamao.

وَحَفِظْنٰهَا مِنْ كُلِّ شَيْطٰنٍ رَّجِيْمٍ ﴿١٨﴾

18. Na Tumeilinda na kila shetani afukuzwaye

اِلَّا مَنِ اسْتَرَقَ السَّمْعَ فَاَتْبَعَهٗ شِهَابٌ مُّبِيْنٌ ﴿١٩﴾

19. Ila yule asikilizaye kwa wizi, basi kinamfuata kijinga king'aacho.

وَالْاَرْضَ مَدَدْنٰهَا وَاَلْقَيْنَا فِيْهَا رَوَاسِيَ وَاَنْۢبَتْنَا فِيْهَا مِنْ كُلِّ شَيْءٍ مَّوْزُوْنٍ ﴿٢٠﴾

20. Na ardhi Tumeitandaza na humo Tumeweka milima na Tumeotesha humo kila kitu kipasacho.

وَجَعَلْنَا لَكُمْ فِيْهَا مَعَايِشَ وَمَنْ لَّسْتُمْ لَهٗ بِرٰزِقِيْنَ ﴿٢١﴾

21. Na Tumewafanyieni humo vitu vya maisha (yenu) na ya yule ambaye ninyi hamumpi riziki.

وَاِنْ مِّنْ شَيْءٍ اِلَّا عِنْدَنَا خَزَآئِنُهٗ ۘ وَمَا نُنَزِّلُهٗٓ اِلَّا بِقَدَرٍ مَّعْلُوْمٍ ﴿٢٢﴾

22. Na hakuna kitu cho chote ila Tunayo hazina yake, wala Hatukiteremshi isipokuwa kwa kipimo maalumu.

وَاَرْسَلْنَا الرِّيٰحَ لَوَاقِحَ فَاَنْزَلْنَا مِنَ السَّمَآءِ مَآءً فَاَسْقَيْنٰكُمُوْهُ ۚ وَمَآ اَنْتُمْ لَهٗ بِخٰزِنِيْنَ ﴿٢٣﴾

23. Na Tunazituma pepo zibebazo (mvuke) na Tunateremsha maji kutoka mawinguni, kisha Tunawanywesheni hayo, wala si ninyi myawekao akiba.

24. Na kwa yakini Sisi ndio Tuhuishao na Tufishao, na Sisi ndio Warithi.

وَاِنَّا لَنَحْنُ نُحْيٖ وَنُمِيْتُ وَنَحْنُ الْوٰرِثُوْنَ ﴿٢٤﴾

25. Na hakika Tunawajua watanguliao katika ninyi, na hakika Tunawajua wachelewao.

وَلَقَدْ عَلِمْنَا الْمُسْتَقْدِمِيْنَ مِنْكُمْ وَلَقَدْ عَلِمْنَا الْمُسْتَاْخِرِيْنَ ﴿٢٥﴾

26. Na bila shaka Mola wako, Yeye ndiye Atawakusanya; hakika Yeye ni Mwenye hekima, Ajuaye.

وَاِنَّ رَبَّكَ هُوَ يَحْشُرُهُمْ ؕ اِنَّهٗ حَكِيْمٌ عَلِيْمٌ ﴿٢٦﴾ ع ٢

FUNGU 3

27. Na bila shaka Tulimwumba mwanadamu kwa udongo utoao sauti, kwa matope meusi yaliyobumbwa.

وَلَقَدْ خَلَقْنَا الْاِنْسَانَ مِنْ صَلْصَالٍ مِّنْ حَمَاٍ مَّسْنُوْنٍ ﴿٢٧﴾

28. Na majinni Tuliwaumba kabla kwa moto wa upepo wenye hari.

وَالْجَآنَّ خَلَقْنٰهُ مِنْ قَبْلُ مِنْ نَّارِ السَّمُوْمِ ﴿٢٨﴾

29. Na (kumbuka) Mola wako Alipowaambia Malaika, Hakika Mimi Nitamwumba mtu kwa udongo utoao sauti, kwa matope meusi yaliyobumbwa.

وَاِذْ قَالَ رَبُّكَ لِلْمَلٰٓئِكَةِ اِنِّيْ خَالِقٌ بَشَرًا مِّنْ صَلْصَالٍ مِّنْ حَمَاٍ مَّسْنُوْنٍ ﴿٢٩﴾

30. Basi Nitakapomkamilisha na kumpulizia roho Yangu, ndipo mmwangukie kumtii.

فَاِذَا سَوَّيْتُهٗ وَنَفَخْتُ فِيْهِ مِنْ رُّوْحِيْ فَقَعُوْا لَهٗ سٰجِدِيْنَ ﴿٣٠﴾

31. Basi Malaika wakatii wote pamoja.

فَسَجَدَ الْمَلٰٓئِكَةُ كُلُّهُمْ اَجْمَعُوْنَ ﴿٣١﴾ لا

32. Isipokuwa Ibilisi, akakataa kuwa pamoja na waliotii.

اِلَّآ اِبْلِيْسَ ؕ اَبٰٓى اَنْ يَّكُوْنَ مَعَ السّٰجِدِيْنَ ﴿٣٢﴾

Aya 28. Watu ambao Mungu hapa anawaita *jinn* (majinni) walikuwa watu wenye tabia ya moto ambao walikuwa wepesi kuhamaki, na hawakuwa wenye kumtii ye yote. Huu ndio mradi wa kuumbwa *kwa moto wa upepo wenye hari.* Kama vile katika sura 21:38 Allah anasema, *Mwanadamu ameumbwa kwa haraka,* na wafasiri wote wanakubaliana kuwa mradi hapa ni tabia ya mwanadamu yenye haraka.

Kwa hakika kabla ya kuzaliwa Adamu watu walikuwa wenye tabia ya moto na wakali kupita kiasi. Adamu alikuwa mtu wa kwanza kufikia hali ya juu ya tabia bora, na hii ndiyo sababu ufunuo wa Allah unaoeleza mwenendo mwema na njia ya watu kukaa pamoja, kwanza aliteremshiwa Adamu, na wafuasi wake wakaondolewa tabia ya moto kwa mafundisho yake, na wakashika tabia ya "udongo" ambao ni kitu kinachoweza kufinyangwa katika umbo lo lote.

33. (Allah) Akasema: Ewe Ibilisi, umekuwaje hukuwa pamoja na waliotii?

قَالَ يٰٓاِبْلِيْسُ مَا لَكَ اَلَّا تَكُوْنَ مَعَ السّٰجِدِيْنَ ﴿٣٣﴾

34. Akasema: Siwezi kumtii mtu uliyemwumba kwa udongo utoao sauti, kwa matope meusi yaliyobumbwa.

قَالَ لَمْ اَكُنْ لِّاَسْجُدَ لِبَشَرٍ خَلَقْتَهٗ مِنْ صَلْصَالٍ مِّنْ حَمَاٍ مَّسْنُوْنٍ ﴿٣٤﴾

35. Akasema: Basi toka humo, maana hakika wewe ndiwe ufukuzwaye.

قَالَ فَاخْرُجْ مِنْهَا فَاِنَّكَ رَجِيْمٌ ۙ﴿٣٥﴾

36. Na kwa yakini itakuwa juu yako laana mpaka siku ya Hukumu.

وَّ اِنَّ عَلَيْكَ اللَّعْنَةَ اِلٰى يَوْمِ الدِّيْنِ ﴿٣٦﴾

37. Akasema: Mola wangu, basi Unipe nafasi mpaka siku watakapofufuliwa.

قَالَ رَبِّ فَاَنْظِرْنِيْٓ اِلٰى يَوْمِ يُبْعَثُوْنَ ﴿٣٧﴾

38. Akasema: Hakika wewe ni katika wale waliopewa nafasi,

قَالَ فَاِنَّكَ مِنَ الْمُنْظَرِيْنَ ۙ﴿٣٨﴾

39. Mpaka siku ya wakati uliowekwa.

اِلٰى يَوْمِ الْوَقْتِ الْمَعْلُوْمِ ﴿٣٩﴾

40. Akasema: Mola wangu, kwa sababu Umenihukumu kupotea, kwa yakini nitawapambia (upotevu) katika ardhi na hakika nitawapoteza wote.

قَالَ رَبِّ بِمَآ اَغْوَيْتَنِيْ لَاُزَيِّنَنَّ لَهُمْ فِي الْاَرْضِ وَلَاُغْوِيَنَّهُمْ اَجْمَعِيْنَ ۙ﴿٤٠﴾

41. Isipokuwa watumishi Wako miongoni mwao waliohalisika.

اِلَّا عِبَادَكَ مِنْهُمُ الْمُخْلَصِيْنَ ﴿٤١﴾

42. (Allah) Akasema: Hii ndiyo njia ya Kwangu iliyonyoka.

قَالَ هٰذَا صِرَاطٌ عَلَيَّ مُسْتَقِيْمٌ ﴿٤٢﴾

43. Hakika watumishi Wangu, wewe hutakuwa na mamlaka juu yao, isipokuwa yule mwenye kukufuata katika wapotevu.

اِنَّ عِبَادِيْ لَيْسَ لَكَ عَلَيْهِمْ سُلْطٰنٌ اِلَّا مَنِ اتَّبَعَكَ مِنَ الْغٰوِيْنَ ﴿٤٣﴾

44. Na bila shaka Jahanamu ndipo mahali pao walipoahidiwa wote.

وَ اِنَّ جَهَنَّمَ لَمَوْعِدُهُمْ اَجْمَعِيْنَ ۙ قف ﴿٤٤﴾

45. Ina milango saba; na kwa kila mlango iko sehemu yao iliyogawanywa.

لَهَا سَبْعَةُ اَبْوَابٍ ؕ لِكُلِّ بَابٍ مِّنْهُمْ جُزْءٌ مَّقْسُوْمٌ ع ﴿٤٥﴾ ع ٣ ١٩ ٣

Aya 39. Siku hiyo ni wakati ambao Mitume na wafuasi wao watapowashinda kabisa washindani wao.

FUNGU 4

46. Kwa hakika wamchao Allah watakuwa katika Mabustani na chemchem.
اِنَّ الْمُتَّقِيْنَ فِيْ جَنّٰتٍ وَّعُيُوْنٍ ۟ؕ ﴿٤٥﴾

47. Ziingieni kwa amani muwe salama.
اُدْخُلُوْهَا بِسَلٰمٍ اٰمِنِيْنَ ﴿٤٦﴾

48. Na Tutaondoa fundo liliomo vifuani mwao, na (watakuwa) ndugu (wakikaa) juu ya viti vya kifalme wakielekeana
وَنَزَعْنَا مَا فِيْ صُدُوْرِهِمْ مِّنْ غِلٍّ اِخْوَانًا عَلٰى سُرُرٍ مُّتَقٰبِلِيْنَ ﴿٤٧﴾

49. Haitawagusa humo taabu wala humo hawatatolewa.
لَا يَمَسُّهُمْ فِيْهَا نَصَبٌ وَّمَا هُمْ مِّنْهَا بِمُخْرَجِيْنَ ﴿٤٨﴾

50. Waambie watumishi Wangu ya kwamba Mimi ni Msamehevu, Mrehemevu.
نَبِّئْ عِبَادِيْٓ اَنِّيْٓ اَنَا الْغَفُوْرُ الرَّحِيْمُ ۙ﴿٤٩﴾

51. Na hakika adhabu Yangu ndiyo adhabu iumizayo.
وَاَنَّ عَذَابِيْ هُوَ الْعَذَابُ الْاَلِيْمُ ﴿٥٠﴾

52. Na uwaambie habari za wageni wa Ibrahimu.
وَنَبِّئْهُمْ عَنْ ضَيْفِ اِبْرٰهِيْمَ ﴿٥١﴾

53. Walipoingia kwake na wakasema, Salaam. Akasema: Kwa hakika sisi tunawaogopeni.
اِذْ دَخَلُوْا عَلَيْهِ فَقَالُوْا سَلٰمًا ؕ قَالَ اِنَّا مِنْكُمْ وَجِلُوْنَ ﴿٥٢﴾

54. Wakasema: Usiogope; kwa yakini sisi tunakupa habari njema ya mtoto mwenye elimu.
قَالُوْا لَا تَوْجَلْ اِنَّا نُبَشِّرُكَ بِغُلٰمٍ عَلِيْمٍ ﴿٥٣﴾

55. Akasema: Je, mnanipa habari njema hali uzee umenishika, basi kwa njia gani mnanipa habari njema?
قَالَ اَبَشَّرْتُمُوْنِيْ عَلٰٓى اَنْ مَّسَّنِيَ الْكِبَرُ فَبِمَ تُبَشِّرُوْنَ ﴿٥٤﴾

56. Wakasema: Tumekupa habari njema iliyo haki, basi usiwe miongoni mwa wakatao tamaa.
قَالُوْا بَشَّرْنٰكَ بِالْحَقِّ فَلَا تَكُنْ مِّنَ الْقٰنِطِيْنَ ﴿٥٥﴾

57. Akasema: Na nani akataye tamaa ya rehema ya Mola wake isipokuwa wale waliopotea?
قَالَ وَمَنْ يَّقْنَطُ مِنْ رَّحْمَةِ رَبِّهٖٓ اِلَّا الضَّآلُّوْنَ ﴿٥٦﴾

58. Akasema: Tena kusudi lenu ni nini enyi mliotumwa?
قَالَ فَمَا خَطْبُكُمْ اَيُّهَا الْمُرْسَلُوْنَ ﴿٥٧﴾

59. Wakasema: Hakika sisi tumetumwa kwa watu wakosefu.
قَالُوْٓا اِنَّآ اُرْسِلْنَآ اِلٰى قَوْمٍ مُّجْرِمِيْنَ ۙ﴿٥٨﴾

إِلَّآ اٰلَ لُوْطٍ ؕ اِنَّا لَمُنَجُّوْهُمْ اَجْمَعِيْنَ ۙ﴿٦٠﴾

60. Isipokuwa wamfuatao Luti. Bila shaka sisi tutawaokoa wote,

اِلَّا امْرَاَتَهٗ ۙ قَدَّرْنَآ ۙ اِنَّهَا لَمِنَ الْغٰبِرِيْنَ ﴿٦١﴾ ع

61. Isipokuwa mkewe. Tunapimia ya kuwa atakuwa miongoni mwa wakaao nyuma.

FUNGU 5

فَلَمَّا جَآءَ اٰلَ لُوْطِ ِالْمُرْسَلُوْنَ ﴿٦٢﴾

62. Basi wajumbe walipofika kwa watu wa Luti,

قَالَ اِنَّكُمْ قَوْمٌ مُّنْكَرُوْنَ ﴿٦٣﴾

63. Akasema: Hakika ninyi ni watu msiojulikana.

قَالُوْا بَلْ جِئْنٰكَ بِمَا كَانُوْا فِيْهِ يَمْتَرُوْنَ ﴿٦٤﴾

64. Wakasema: Bali sisi tumekuletea yale ambayo walikuwa wanayafanyia shaka.

وَ اَتَيْنٰكَ بِالْحَقِّ وَ اِنَّا لَصٰدِقُوْنَ ﴿٦٥﴾

65. Na tumefika kwako kwa haki, na hakika sisi ni wasemao kweli.

فَاَسْرِ بِاَهْلِكَ بِقِطْعٍ مِّنَ الَّيْلِ وَاتَّبِعْ اَدْبَارَهُمْ وَلَا يَلْتَفِتْ مِنْكُمْ اَحَدٌ وَّامْضُوْا حَيْثُ تُؤْمَرُوْنَ ﴿٦٦﴾

66. Basi safiri na ahali zako katika kipande cha usiku, na wewe ufuate nyuma yao; wala mmoja wenu asigeuke nyuma, na mwende mnapoamrishwa.

وَقَضَيْنَآ اِلَيْهِ ذٰلِكَ الْاَمْرَ اَنَّ دَابِرَ هٰٓؤُلَآءِ مَقْطُوْعٌ مُّصْبِحِيْنَ ﴿٦٧﴾

67. Na Tukamkatia jambo hili ya kwamba mizizi yao itakatwa asubuhi.

وَجَآءَ اَهْلُ الْمَدِيْنَةِ يَسْتَبْشِرُوْنَ ﴿٦٨﴾

68. Na wakaja watu wa mji wakifurahi.

قَالَ اِنَّ هٰٓؤُلَآءِ ضَيْفِيْ فَلَا تَفْضَحُوْنِ ۙ﴿٦٩﴾

69. Akasema: Hakika hawa ni wageni wangu, kwa hiyo msinifedheheshe.

وَاتَّقُوا اللّٰهَ وَلَا تُخْزُوْنِ ﴿٧٠﴾

70. Na Mwogopeni Allah wala msinidhalilishe.

Aya 63. *Watu msiojulikana,* yaani wageni au wasafiri.

Aya 66. *Asigeuke nyuma,* yaani asijali habari za watu watakaoangamia ambao mtawaacha nyuma yenu.

Aya 68. *Wakifurahi,* yaani wakifurahi kuwa sasa wamepata sababu ya kumfukuzia Nabii Luti katika mji wao, maana walikwisha mkataza zamani asilete wageni, kwa vile wao walikuwa katika hali ya vita na majirani zao. Na kwa kuwa walikwisha choka na mahubiri yake, wasiweze kumfukuza bila sababu kwa vile naye ni mwenyeji pale na binti zake wameolewa hapo hapo. Sasa wakafurahi kuona wamepata kisa cha kutosha kumfukuzia. Siyo kama wasemavyo watu kuwa walifurahi maana walifikiri kuwa wamepata nafasi ya kuwafira wageni wa Nabii Luti.

71. Wakasema: Je sisi hatukukukataza (kukaribisha) watu (wa nje)?

قَالُوْٓا اَوَلَمْ نَنْهَكَ عَنِ الْعٰلَمِيْنَ ﴿٧١﴾

72. Akasema, "(Hebu waoneeni haya) hawa binti zangu kama nyinyi ni wenye kuchukua hatua yoyote.

قَالَ هٰٓؤُلَآءِ بَنٰتِيْٓ اِنْ كُنْتُمْ فٰعِلِيْنَ ﴿٧٢﴾

73. Kwa kiapo cha maisha yako, hakika wao katika ulevi wao wanahangaika ovyo.

لَعَمْرُكَ اِنَّهُمْ لَفِيْ سَكْرَتِهِمْ يَعْمَهُوْنَ ﴿٧٣﴾

74. Mara adhabu yenye mngurumo ikawakamata lilipotoka jua.

فَاَخَذَتْهُمُ الصَّيْحَةُ مُشْرِقِيْنَ ﴿٧٤﴾

75. Basi Tukaufanya (mji ule) juu yake kuwa chini yake; na Tukawapigishia mvua ya mawe ya udongo.

فَجَعَلْنَا عَالِيَهَا سَافِلَهَا وَاَمْطَرْنَا عَلَيْهِمْ حِجَارَةً مِّنْ سِجِّيْلٍ ﴿٧٥﴾

76. Hakika katika hayo zimo Ishara kwa watu wenye busara.

اِنَّ فِيْ ذٰلِكَ لَاٰيٰتٍ لِّلْمُتَوَسِّمِيْنَ ﴿٧٦﴾

77. Na (mji) huo upo penye barabara ipitwayo.

وَاِنَّهَا لَبِسَبِيْلٍ مُّقِيْمٍ ﴿٧٧﴾

78. Bila shaka katika hayo zimo Ishara kwa waaminio.

اِنَّ فِيْ ذٰلِكَ لَاٰيَةً لِّلْمُؤْمِنِيْنَ ﴿٧٨﴾

79. Na hakika watu wa Kichaka (pia) walikuwa wadhalimu.

وَاِنْ كَانَ اَصْحٰبُ الْاَيْكَةِ لَظٰلِمِيْنَ ﴿٧٩﴾

80. Kwa hiyo Tukawaadhibu; na (miji) hiyo miwili iko kwenye barabara iliyo wazi.

فَانْتَقَمْنَا مِنْهُمْ ۘ وَاِنَّهُمَا لَبِاِمَامٍ مُّبِيْنٍ ﴿٨٠﴾

FUNGU 6

81. Na bila shaka wenyeji wa Hijri (pia) waliwakadhibisha Mitume.

وَلَقَدْ كَذَّبَ اَصْحٰبُ الْحِجْرِ الْمُرْسَلِيْنَ ﴿٨١﴾

82. Na Tuliwapa Ishara Zetu, lakini walikuwa wakizipuuza.

وَاٰتَيْنٰهُمْ اٰيٰتِنَا فَكَانُوْا عَنْهَا مُعْرِضِيْنَ ﴿٨٢﴾

Aya 75. Majumba ya watu wa Nabii Luti yalipinduliwa. Tetemeko kali la nchi liliwafikia, likaiinua ardhi na kuwafukia.

Aya 79. *Aikat.* Neno hili linaonekana kuwa linahusu nchi ya Madiani.

Aya 81. *Hijr* ni mji uliokuwa baina ya Tabuk na Madina. Watu wa Thamud waliishi hapo na Nabii Saleh ndiye aliyetumwa kwao.

وَكَانُوْا يَنْحِتُوْنَ مِنَ الْجِبَالِ بُيُوْتًا اٰمِنِيْنَ ﴿٨٢﴾

83. Nao walikuwa wakichonga majumba katika majabali kwa amani.

فَاَخَذَتْهُمُ الصَّيْحَةُ مُصْبِحِيْنَ ﴿٨٣﴾

84. Basi adhabu yenye mngurumo ikawafikia asubuhi.

فَمَآ اَغْنٰى عَنْهُمْ مَّا كَانُوْا يَكْسِبُوْنَ ﴿٨٤﴾

85. Na hayakuwafaa waliyokuwa wakiyachuma.

وَمَا خَلَقْنَا السَّمٰوٰتِ وَالْاَرْضَ وَمَا بَيْنَهُمَآ اِلَّا بِالْحَقِّ ؕ وَاِنَّ السَّاعَةَ لَاٰتِيَةٌ فَاصْفَحِ الصَّفْحَ الْجَمِيْلَ ﴿٨٥﴾

86. Na Hatukuziumba mbingu na ardhi na vilivyomo kati yao ila kwa haki; na bila shaka saa inafika, basi samehe (makosa yao) msamaha mwema.

اِنَّ رَبَّكَ هُوَ الْخَلّٰقُ الْعَلِيْمُ ﴿٨٦﴾

87. Hakika Mola wako ndiye Mwumbaji mkuu, Mjuzi.

وَلَقَدْ اٰتَيْنٰكَ سَبْعًا مِّنَ الْمَثَانِيْ وَالْقُرْاٰنَ الْعَظِيْمَ ﴿٨٧﴾

88. Na kwa yakini Tumekwisha kupa (Aya) saba zisomwazo mara kwa mara na Qur'an kubwa.

لَا تَمُدَّنَّ عَيْنَيْكَ اِلٰى مَا مَتَّعْنَا بِهٖۤ اَزْوَاجًا مِّنْهُمْ وَلَا تَحْزَنْ عَلَيْهِمْ وَاخْفِضْ جَنَاحَكَ لِلْمُؤْمِنِيْنَ ﴿٨٨﴾

89. Usizinyooshee macho yako (kwa choyo) zile neema za kupita Tulizowapa baadhi ya makundi miongoni mwao, wala usiwahuzunikie; na inamisha bawa lako (la huruma) kwa waaminio.

وَقُلْ اِنِّيْۤ اَنَا النَّذِيْرُ الْمُبِيْنُ ﴿٨٩﴾

90. Na sema: Hakika mimi ndimi Mwonyaji dhahiri,

كَمَآ اَنْزَلْنَا عَلَى الْمُقْتَسِمِيْنَ ﴿٩٠﴾

91. (wa ile adhabu) Kama Tulivyowateremshia waliojigawa makundi makundi.

الَّذِيْنَ جَعَلُوا الْقُرْاٰنَ عِضِيْنَ ﴿٩١﴾

92. Ambao wameigawa Kurani vipande vipande.

Aya 86. *Saa,* Neno hili linahusu saa ya siku ya Hukumu na pia wakati uliowekwa kwa ajili ya kuadhibiwa maadui wanaoiadui haki na kushinda kwa waaminio

Aya 88. Aya saba zinazosomwa mara kwa mara ni sura ya Alhamdu. Seyidna Umar, Seyidna Ali, Ibni Abbas na Ibni Mas'ud wote wanakubali hivi na kadhalika Zajjaj na Abu Hayyan.

Aya 92. Wakati mwingine aya hii hutafsiriwa kwa wakati ujao badala ya wakati uliopita kwa sababu aya hizi zimebeba onyo kali kwa ajili ya Waislamu. Hakuna ajabu yo yote kwa wakati uliopita kutumika kwa kuashiria wakati ujao, kwa sababu, nyingi miongoni mwa tabiri za namna hiyo ambazo ni lazima kabisa zitokee, zimeelezwa kwa wakati uliopita ndani ya Qur'an Tukufu. Wakati uliopita haubadiliki. Tabiri zinazosomeka kwa wakati uliopita zinatilia mkazo uhakika. Hivyo basi tafsiri yatakiwa itiririke kama ifuatavyo:

فَوَرَبِّكَ لَنَسْـَٔلَنَّهُمْ اَجْمَعِيْنَ ﴿٩٣﴾

93. Na kwa haki ya Mola wako, bila shaka sisi Tutawauliza wao wote.

عَمَّا كَانُوْا يَعْمَلُوْنَ ﴿٩٤﴾

94. Juu ya yale waliyokuwa wakiyatenda.

فَاصْدَعْ بِمَا تُؤْمَرُ وَاَعْرِضْ عَنِ الْمُشْرِكِيْنَ ﴿٩٥﴾

95. Basi uyatangaze uliyoamrishwa na ujitenge mbali na washirikina.

اِنَّا كَفَيْنٰكَ الْمُسْتَهْزِءِيْنَ ﴿٩٦﴾

96. Hakika Sisi Tunakutosha kwa (shari ya) wafanyao dhihaka.

الَّذِيْنَ يَجْعَلُوْنَ مَعَ اللّٰهِ اِلٰهًا اٰخَرَ ۚ فَسَوْفَ يَعْلَمُوْنَ ﴿٩٧﴾

97. Ambao wanaweka pamoja na Allah, mungu mwingine, basi hivi karibuni watajua.

وَلَقَدْ نَعْلَمُ اَنَّكَ يَضِيْقُ صَدْرُكَ بِمَا يَقُوْلُوْنَ ﴿٩٨﴾

98. Na kwa yakini Sisi Tunajua ya kwamba kifua chako kinadhikika kwa yale wasemayo.

فَسَبِّحْ بِحَمْدِ رَبِّكَ وَكُنْ مِّنَ السّٰجِدِيْنَ ﴿٩٩﴾

99. Basi Mtukuze Mola wako kwa sifa njema, na uwe miongoni mwa wanaosujudu.

وَاعْبُدْ رَبَّكَ حَتّٰى يَاْتِيَكَ الْيَقِيْنُ ﴿١٠٠﴾

100. Na umwabudu Mola wako mpaka ikufikie mauti.

"Na kwa yakini Tumekwisha kupa aya saba zisomwazo mara kwa mara na Qur'an kubwa. Usizinyooshee macho yako kwa choyo zile neema za kupita Tulizowapa baadhi ya makundi miongoni mwao, wala usiwahuzunikie; na inamisha bawa lako la huruma kwa waaminio. Na sema: Hakika mimi ndimi Mwonyaji dhahiri. Kama ilivyo ada, "Tutawateremshia adhabu wale ambao watajigawa makundi-makundi na ambao wataigawanya Qur'an vipande-vipande."

Tafisiri hii inabainika kuwa yenye kufaa zaidi tunapoyaweka mbele ya macho yetu maudhui ya aya hizi na kugundua kwamba aya zilizotangulia zinaanza na utangulizi bayana wa Qur'an Tukufu kuwa ni Kitabu kilichotukuka. Kwa hiyo wote wale ambao, ingawa wanadai kuwa watiifu wa Qur'an lakini wanaupuuza ujumbe wake wa msingi wa umoja, na wanajigawa vikundi vikundi na ili kuthibitisha kwamba tafsiri yao ndiyo sahihi wanaishia katika kuigawa Quran vipande-vipande; kila kundi likiwa limezing'ang'ania baadhi ya aya na kuzitafsiri kwa kukidhi maslahi yao yaliyo kinyume na wengine ambao nao huzing'ang'ania baadhi ya aya na kuzitafsiri kulingana na maslahi yao. Mgawanyiko huu waelezwa kuwa ni mkali sana na wa mwisho hivi kwamba hakuna uwezekano uliobakia wa kuleta muafaka baina ya vikundi mbalimbali vinavyopinzana. Hii inasababisha watu wa umati mmoja kugawanyika katika madhehebu na kwa utaratibu huo huo, kuigawanya Qur'an vipande vipande.

Aya 99. Aya hii mradi wake ni kwamba kwa kuwa wakati wa mafanikio unakuja, Mtume *s.a.w.* apitishe wakati wake zaidi kwa kusali bila kuzuiwa na maadui zake ambao hawatakuwa na uwezo wa kumwingilia katika kazi yake.

سُوْرَةُ النَّحْلِ مَكِّيَّةٌ وَّ هِيَ مَعَ الْبَسْمَلَةِ مِائَةٌ وَّ تِسْعٌ وَّ عِشْرُوْنَ اٰيَةً وَّ سِتَّةَ عَشَرَ رُكُوْعًا

16 SURA AN-NAHL

Imeteremshwa Makka

Ina mafungu 16 na Aya 129 pamoja na Bismillahi

بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ ①

1. Kwa jina la Allah, Mwingi wa rehema, Mwingi wa ukarimu.

اَتٰۤى اَمْرُ اللّٰهِ فَلَا تَسْتَعْجِلُوْهُ ؕ سُبْحٰنَهٗ وَ تَعٰلٰى عَمَّا يُشْرِكُوْنَ ②

2. Amri ya Allah imefika, basi msiiharakishie; Yeye ni Mtakatifu, na Yu juu kuliko wanavyovishirikisha.

يُنَزِّلُ الْمَلٰٓئِكَةَ بِالرُّوْحِ مِنْ اَمْرِهٖ عَلٰى مَنْ يَّشَآءُ مِنْ عِبَادِهٖۤ اَنْ اَنْذِرُوْۤا اَنَّهٗ لَاۤ اِلٰهَ اِلَّاۤ اَنَا فَاتَّقُوْنِ ③

3. Huwateremsha Malaika kwa amri Yake wakiwa na wahyi kwa ye yote Amtakaye miongoni mwa watumishi Wake Akisema: Onyeni kwamba hakuna Mungu isipokuwa Mimi; kwa hiyo nicheni Mimi tu.

خَلَقَ السَّمٰوٰتِ وَ الْاَرْضَ بِالْحَقِّ ؕ تَعٰلٰى عَمَّا يُشْرِكُوْنَ ④

4. Ameziumba mbingu na ardhi kwa haki; Yu juu kuliko wale wanaowashirikisha.

خَلَقَ الْاِنْسَانَ مِنْ نُّطْفَةٍ فَاِذَا هُوَ خَصِيْمٌ مُّبِيْنٌ ⑤

5. Amemwumba mwanadamu kwa tone la manii, lakini mara amekuwa mgomvi dhahiri.

Baadhi ya wafasiri wanasema ya kuwa sura hii yote ilishuka Makka. Lakini wengine kama Ibni Abbas wanasema ya kuwa Aya 96, 97 na 98 zilishuka Madina. Lakini wanazuoni wengine wanasema Aya zilizoshuka Madina ni 127, 128 na 129, hali wengine wanasema, Aya hizo ni 111, 127 na 128, bado kuna wengine wanaosema Aya hizo ni 2, 3, na 4. Lakini Katada anasema sura yote ni ya Madina isipokuwa Aya 2, 3, na 4.

Sura hii imeitwa *An-Nahl* (Nyuki) kwa sababu imetaja silika ya asili ya nyuki ambayo imeitwa wahyi (ufunuo) katika Qur'an kwa kufahamisha ya kuwa ulimwengu wote unategemea wahyi ili uendelee vizuri, uwe wahyi wa dhahiri au wa siri.

Aya 2. *Amri ya Allah imefika,* mradi wake: (1) wakati wa adhabu ya wasioamini umefika; au (2) wakati wa kuleta mpango mpya umefika.

Aya 3. *Ruuh,* "ufunuo," mradi wake ni neno la Mungu linalotia uhai. Pia neno hili hutumika kuonyesha ujumbe aliotumwa nao Nabii kwa kuwa unatia uzima wa kiroho.

Katika watumishi Wake, yaani watumishi wateule wa Allah, siyo watumishi wo wote; na yanaonyesha kuwa utume ni kipawa maalum ambacho hupewa watumishi Wake tu.

وَالْاَنْعَامَ خَلَقَهَا ۚ لَكُمْ فِيْهَا دِفْءٌ
وَّمَنَافِعُ وَمِنْهَا تَاْكُلُوْنَ ۝٦

6. Na pia Amewaumba wanyama, katika hao mnapata (vifaa vitiavyo) joto na manufaa (mengine), na wengine mnakula.

وَلَكُمْ فِيْهَا جَمَالٌ حِيْنَ تُرِيْحُوْنَ
وَحِيْنَ تَسْرَحُوْنَ ۝٧

7. Na katika hao ni uzuri kwenu mnapowarudisha jioni na mnapowapeleka malishoni asubuhi.

وَتَحْمِلُ اَثْقَالَكُمْ اِلٰى بَلَدٍ لَّمْ تَكُوْنُوْا
بٰلِغِيْهِ اِلَّا بِشِقِّ الْاَنْفُسِ ؕ اِنَّ رَبَّكُمْ
لَرَءُوْفٌ رَّحِيْمٌ ۝٨

8. Na hubeba mizigo yenu kupeleka kwenye mji msikoweza kufika isipokuwa kwa kujitia taabu. Hakika Mola wenu ni Mpole sana, Mrehemevu.

وَّالْخَيْلَ وَالْبِغَالَ وَالْحَمِيْرَ لِتَرْكَبُوْهَا
وَزِيْنَةً ؕ وَيَخْلُقُ مَا لَا تَعْلَمُوْنَ ۝٩

9. Na (Amewaumba) farasi na nyumbu na punda ili mwapande na (wawe) mapambo, na Ataumba msivyovijua.

وَعَلَى اللّٰهِ قَصْدُ السَّبِيْلِ وَمِنْهَا جَآئِرٌ ؕ
وَلَوْ شَآءَ لَهَدٰىكُمْ اَجْمَعِيْنَ ۝١٠

10. Na ni juu ya Allah (kuonyesha) njia iliyo sawa, na ziko (njia) zingine zisizo sawa. Na kama Angalipenda, bila shaka Angaliwaongozeni ninyi nyote.

FUNGU 2

هُوَ الَّذِيْٓ اَنْزَلَ مِنَ السَّمَآءِ مَآءً لَّكُمْ مِّنْهُ
شَرَابٌ وَّمِنْهُ شَجَرٌ فِيْهِ تُسِيْمُوْنَ ۝١١

11. Yeye ndiye Huwateremshieni maji kutoka mawinguni; kwayo mnapata kinywaji, na kwayo (inaota) miti ambayo humo mnalisha (wanyama).

يُنْۢبِتُ لَكُمْ بِهِ الزَّرْعَ وَالزَّيْتُوْنَ
وَالنَّخِيْلَ وَالْاَعْنَابَ وَمِنْ كُلِّ الثَّمَرٰتِ ؕ
اِنَّ فِيْ ذٰلِكَ لَاٰيَةً لِّقَوْمٍ يَّتَفَكَّرُوْنَ ۝١٢

12. Kwayo Huwaotesheeni mimea ya kila aina na mizeituni na mitende na mizabibu na kila matunda. Bila shaka katika hayo imo ishara kwa watu wenye kutafakari.

وَسَخَّرَ لَكُمُ الَّيْلَ وَالنَّهَارَ ۙ وَالشَّمْسَ
وَالْقَمَرَ ؕ وَالنُّجُوْمُ مُسَخَّرٰتٌۢ
بِاَمْرِهٖ ؕ اِنَّ فِيْ ذٰلِكَ لَاٰيٰتٍ لِّقَوْمٍ
يَّعْقِلُوْنَ ۝١٣

13. Na Amewatiishieni usiku na mchana, na jua na mwezi, na (pia) nyota zimetiishwa kwa amri Yake. Hakika katika hayo zimo Ishara kwa watu wenye akili.

Aya 9. *Ataviumba msivyovijua.* Hii ni bishara ya kutokea duniani vitu vingi vyenye raha zaidi vya kusafiria nayo imetimia kwa ajabu sana, na itaendelea kila siku kutimia.

وَمَا ذَرَاَ لَكُمْ فِي الْاَرْضِ مُخْتَلِفًا اَلْوَانُهٗ ؕ اِنَّ فِيْ ذٰلِكَ لَاٰيَةً لِّقَوْمٍ يَّذَّكَّرُوْنَ ﴿١٤﴾

14. Na Alivyowaumbieni katika ardhi vya rangi mbalimbali (vinawatiini). Hakika katika hayo imo Ishara kwa watu washikao nasaha.

وَهُوَ الَّذِيْ سَخَّرَ الْبَحْرَ لِتَاْكُلُوْا مِنْهُ لَحْمًا طَرِيًّا وَّتَسْتَخْرِجُوْا مِنْهُ حِلْيَةً تَلْبَسُوْنَهَا ۚ وَتَرَى الْفُلْكَ مَوَاخِرَ فِيْهِ وَ لِتَبْتَغُوْا مِنْ فَضْلِهٖ وَلَعَلَّكُمْ تَشْكُرُوْنَ ﴿١٥﴾

15. Na Yeye ndiye Ameitiisha bahari ili humo mle nyama mbichi, na mtoe humo mapambo mnayovaa. Na utaona merikebu zikipasua humo, na ili mtafute fadhili Zake, na ili mpate kushukuru.

وَاَلْقٰى فِي الْاَرْضِ رَوَاسِيَ اَنْ تَمِيْدَ بِكُمْ وَاَنْهٰرًا وَّ سُبُلًا لَّعَلَّكُمْ تَهْتَدُوْنَ ﴿١٦﴾ ۙ

16. Na Akaweka katika ardhi milima madhubuti ili mpate mahitajio ya vyakula, na pia mito na mabarabara ili mpate kuongoka.

وَعَلٰمٰتٍ ؕ وَبِالنَّجْمِ هُمْ يَهْتَدُوْنَ ﴿١٧﴾

17. Na (Ameziweka) alama, na kwa nyota (pia) wao wanafuata njia.

اَفَمَنْ يَّخْلُقُ كَمَنْ لَّا يَخْلُقُ ؕ اَفَلَا تَذَكَّرُوْنَ ﴿١٨﴾

18. Ati, yule Anayeumba Anaweza kuwa sawa na asiyeumba? Je, hamshiki nasaha?

وَ اِنْ تَعُدُّوْا نِعْمَةَ اللّٰهِ لَا تُحْصُوْهَا ؕ اِنَّ اللّٰهَ لَغَفُوْرٌ رَّحِيْمٌ ﴿١٩﴾

19. Na mkihesabu neema za Allah hamtaweza kuzihesabu. Hakika Allah ni Msamehevu sana Mrehemevu.

وَاللّٰهُ يَعْلَمُ مَا تُسِرُّوْنَ وَمَا تُعْلِنُوْنَ ﴿٢٠﴾

20. Na Allah Huyajua mnayoyaficha na mnayoyadhihirisha.

وَالَّذِيْنَ يَدْعُوْنَ مِنْ دُوْنِ اللّٰهِ لَا يَخْلُقُوْنَ شَيْـًٔا وَّهُمْ يُخْلَقُوْنَ ﴿٢١﴾ ؕ

21. Na wale ambao wanawaita badala ya Allah hawaumbi cho chote, bali wao wameumbwa;

Aya 16. Wanazuoni wengi wameyatafsiri maneno *an tamiida bikum* kuwa ni tetemeko ambapo kama itakubalika hivyo itakuwa na maana kwamba Allah anazihesabu neema zake kwa binadamu kwa kuwakumbusha kwamba "Tumeiumba milima ili kusababisha matetemeko ya ardhi yatakayoleta uharibifu huku na kule. Kwa bahati mbaya imepuuzwa kwamba neno *tamiida* linatokana na nneo *maada* ambalo lina maana ya kupatia chakula. Neno *maaidah* lililotumika katika Qur'an Tukufu linatokana na nneo hilo hilo *maada*. Tukiwa na maana hii mbele ya macho yetu, uelewa wote kabisa wa aya hii utabadilika. Itamkumbusha binadamu kwamba Allah Ameiumba milima ambayo ni muhimu kwa ajili ya kuvipatia chakula viumbe vyote vyenye uhai. Mara kwa mara maji hunyanyuliwa kutoka katika maziwa, bahari ndogo na bahari kubwa kwa njia ya mvuke na kupelekwa kwenye miinuko ya juu ambako hugandishwa katika chembe chembe zilizo kubwa kuliko za mvuke. Kuwepo kwa milima ni jambo la muhimu kwa

اَمْوَاتٌ غَيْرُ اَحْيَآءٍ ۚ وَمَا يَشْعُرُوْنَ ۙ اَيَّانَ يُبْعَثُوْنَ ﴿٢١﴾ ع ٨

22. Ni wafu, si wazima, na hawajui watafufuliwa lini.

FUNGU 3

اِلٰهُكُمْ اِلٰهٌ وَّاحِدٌ ۚ فَالَّذِيْنَ لَا يُؤْمِنُوْنَ بِالْاٰخِرَةِ قُلُوْبُهُمْ مُّنْكِرَةٌ وَّ هُمْ مُّسْتَكْبِرُوْنَ ﴿٢٢﴾

23. Mungu wenu ni Mungu Mmoja; lakini wale wasioiamini Akhera mioyo yao inakataa nao wanatakabari.

لَا جَرَمَ اَنَّ اللّٰهَ يَعْلَمُ مَا يُسِرُّوْنَ وَمَا يُعْلِنُوْنَ ؕ اِنَّهٗ لَا يُحِبُّ الْمُسْتَكْبِرِيْنَ ﴿٢٣﴾

24. Bila shaka Allah Anayajua wanayoyaficha na wanayoyadhihirisha. Kwa hakika Yeye Hawapendi wanaotakabari.

وَ اِذَا قِيْلَ لَهُمْ مَّاذَاۤ اَنْزَلَ رَبُّكُمْ ۙ قَالُوْۤا اَسَاطِيْرُ الْاَوَّلِيْنَ ﴿٢٤﴾ ۙ

25. Na wanapoambiwa: Mola wenu Ameteremsha nini? Wanasema: Hadithi za (watu) wa zamani.

لِيَحْمِلُوْۤا اَوْزَارَهُمْ كَامِلَةً يَّوْمَ الْقِيٰمَةِ ۙ وَمِنْ اَوْزَارِ الَّذِيْنَ يُضِلُّوْنَهُمْ بِغَيْرِ عِلْمٍ ؕ اَلَا سَآءَ مَا يَزِرُوْنَ ﴿٢٥﴾ ع ٩

26. Ili wabebe mizigo yao kamili siku ya Kiyama, na (pia) sehemu ya mizigo ya wale wanaowapoteza bila ya elimu. Sikilizeni! ni mabaya wanayobeba.

FUNGU 4

قَدْ مَكَرَ الَّذِيْنَ مِنْ قَبْلِهِمْ فَاَتَى اللّٰهُ بُنْيَانَهُمْ مِّنَ الْقَوَاعِدِ فَخَرَّ عَلَيْهِمُ السَّقْفُ مِنْ فَوْقِهِمْ وَاَتٰىهُمُ الْعَذَابُ مِنْ حَيْثُ لَا يَشْعُرُوْنَ ﴿٢٦﴾

27. Walifanya hila wale waliokuwa kabla yao, basi Allah Akazifikia nyumba zao kwenye misingi, ndipo dari zikawaangukia kutoka juu yao; na ikawafikia adhabu kutoka wasipopajua.

---

ajili ya kugeuza mvuke urejee tena kwenye hali ya kuwa maji na kuzalisha mvua za mtandao mpana ambazo hurejeshwa tena ardhini na kusababisha mizunguko mikubwa ya chakula. Tafsiri hii ndiyo iliyo ya pekee inayokaa sawa katika maudhui na inakubaliana kikamilifu na sehemu iliyobakia ya aya hii. Kwa hiyo maana sahihi itakuwa: "Amesimika milima juu ya ardhi ili awapatieni chakula, na mito na mabarabara ili mpate kuongoka." Uhusiano wa maji na chakula ni jambo lililo wazi. Katika historia ya Ustaarabu mito ndiyo iliyokuwa imefanya kazi ya muhimu ya kuwezesha kuwapo kwa milima na mbuga na njia zilijengwa kando kando ya mito.

Aya 22. Aya hii inaonyesha ya kuwa miungu yote iliyokuwa inaabudiwa wakati iliposhuka Qur'an ilikuwa imekufa. Basi kama Nabiii Isa aliyekuwa anaabudiwa na Wakristo toka kabla ya wakati huo alikuwa hajafa, hapo tena yeye italazimu aonekane kuwa Mungu wa haki, na hii ni kufuru kubwa kabisa. Hivyo Nabii Isa si hai, amekwisha kufa.

ثُمَّ يَوْمَ الْقِيٰمَةِ يُخْزِيْهِمْ وَيَقُوْلُ اَيْنَ
شُرَكَآءِيَ الَّذِيْنَ كُنْتُمْ تُشَآقُّوْنَ فِيْهِمْ ؕ
قَالَ الَّذِيْنَ اُوْتُوا الْعِلْمَ اِنَّ الْخِزْيَ
الْيَوْمَ وَالسُّوْٓءَ عَلَى الْكٰفِرِيْنَ ۙ﴿۲۸﴾
الَّذِيْنَ تَتَوَفّٰىهُمُ الْمَلٰٓئِكَةُ ظَالِمِيْٓ
اَنْفُسِهِمْ ۠ فَاَلْقَوُا السَّلَمَ مَا كُنَّا نَعْمَلُ
مِنْ سُوْٓءٍ ؕ بَلٰٓى اِنَّ اللّٰهَ عَلِيْمٌۢ بِمَا كُنْتُمْ
تَعْمَلُوْنَ ﴿۲۹﴾
فَادْخُلُوْٓا اَبْوَابَ جَهَنَّمَ خٰلِدِيْنَ فِيْهَا ؕ
فَلَبِئْسَ مَثْوَى الْمُتَكَبِّرِيْنَ ﴿۳۰﴾
وَقِيْلَ لِلَّذِيْنَ اتَّقَوْا مَاذَآ اَنْزَلَ رَبُّكُمْ ؕ
قَالُوْا خَيْرًا ؕ لِلَّذِيْنَ اَحْسَنُوْا فِيْ هٰذِهِ الدُّنْيَا
حَسَنَةٌ ؕ وَلَدَارُ الْاٰخِرَةِ خَيْرٌ ؕ وَلَنِعْمَ
دَارُ الْمُتَّقِيْنَ ۙ﴿۳۱﴾
جَنّٰتُ عَدْنٍ يَّدْخُلُوْنَهَا تَجْرِيْ مِنْ تَحْتِهَا
الْاَنْهٰرُ لَهُمْ فِيْهَا مَا يَشَآءُوْنَ ؕ كَذٰلِكَ
يَجْزِي اللّٰهُ الْمُتَّقِيْنَ ۙ﴿۳۲﴾
الَّذِيْنَ تَتَوَفّٰىهُمُ الْمَلٰٓئِكَةُ طَيِّبِيْنَ ۙ
يَقُوْلُوْنَ سَلٰمٌ عَلَيْكُمُ ۙ ادْخُلُوا الْجَنَّةَ بِمَا
كُنْتُمْ تَعْمَلُوْنَ ﴿۳۳﴾
هَلْ يَنْظُرُوْنَ اِلَّآ اَنْ تَاْتِيَهُمُ الْمَلٰٓئِكَةُ
اَوْ يَاْتِيَ اَمْرُ رَبِّكَ ؕ كَذٰلِكَ فَعَلَ الَّذِيْنَ
مِنْ قَبْلِهِمْ ؕ وَمَا ظَلَمَهُمُ اللّٰهُ
وَلٰكِنْ كَانُوْٓا اَنْفُسَهُمْ يَظْلِمُوْنَ ﴿۳۴﴾

28. Kisha siku ya Kiyama Atawafedhehesha na Atasema: Wako wapi washirika Wangu ambao kwa ajili yao mlikuwa mkigombana (na Manabii)? Watasema wale walipewa elimu: Hakika fedheha na msiba leo vitawafikia makafiri,

29. Ambao Malaika huwafisha hali wamejidhulumu nafsi zao. Basi watatoa amani (wakisema): Hatukuwa tukifanya uovu wo wote. Naam, hakika Allah Anayajua sana mliyokuwa mkitenda.

30. Kwa hiyo ingieni milango ya Jahanamu kwa kukaa humo. Basi ni baya sana kao la wafanyao kiburi.

31. Na wanaambiwa wale walioshika utawa: Ni nini Aliyoteremsha Mola wenu? Wanasema: Heri. Ama wale waliofanya wema katika dunia hii watapata wema, na hakika nyumba ya Akhera ni nzuri; na ni bora kabisa nyumba ya washikao utawa.

32. Bustani za milele wataziingia; inapita ndani yake mito; humo watapata watakacho. Hivi ndivyo Allah Awalipavyo washikao utawa.

33. Wale ambao Malaika huwafisha wanapokuwa katika hali njema, watasema: Amani iwe juu yenu; ingieni Peponi kwa sababu ya yale mliyokuwa mkiyatenda.

34. Hawangoji ila Malaika wawafikie au iwafikie amri ya Mola wako. Kama hivyo walifanya wale waliokuwa kabla yao. Na Allah Hakuwadhulumu, lakini walikuwa wamejidhulumu wenyewe.

Aya 34. Malaika au amri ya Mungu kufika, muradi wake ni kufika adhabu.

فَاَصَابَهُمْ سَيِّاٰتُ مَا عَمِلُوْا وَحَاقَ بِهِمْ مَّا كَانُوْا بِهٖ يَسْتَهْزِءُوْنَ ﴿٣٥﴾ ع ١٤

35. Basi ukawafikia uovu wa yale waliyoyafanya na ikawazunguka (adhabu) waliyokuwa wakiifanyia mzaha.

FUNGU 5

وَقَالَ الَّذِيْنَ اَشْرَكُوْا لَوْ شَآءَ اللّٰهُ مَا عَبَدْنَا مِنْ دُوْنِهٖ مِنْ شَيْءٍ نَّحْنُ وَلَآ اٰبَآؤُنَا وَلَا حَرَّمْنَا مِنْ دُوْنِهٖ مِنْ شَيْءٍ ؕ كَذٰلِكَ فَعَلَ الَّذِيْنَ مِنْ قَبْلِهِمْ ۚ فَهَلْ عَلَى الرُّسُلِ اِلَّا الْبَلٰغُ الْمُبِيْنُ ﴿٣٦﴾

36. Na wale walioshirikisha watasema: Kama Angalipenda Allah, Tusingaliabudu cho chote badala Yake, sisi wala baba zetu, wala tusingaliharimisha cho chote bila Yeye (kutoa amri). Kama hivyo walifanya wale waliokuwa kabla yao. Basi si kazi ya Mitume isipokuwa kufikisha (ujumbe) waziwazi.

وَلَقَدْ بَعَثْنَا فِيْ كُلِّ اُمَّةٍ رَّسُوْلًا اَنِ اعْبُدُوا اللّٰهَ وَاجْتَنِبُوا الطَّاغُوْتَ ۚ فَمِنْهُمْ مَّنْ هَدَى اللّٰهُ وَمِنْهُمْ مَّنْ حَقَّتْ عَلَيْهِ الضَّلٰلَةُ ؕ فَسِيْرُوْا فِي الْاَرْضِ فَانْظُرُوْا كَيْفَ كَانَ عَاقِبَةُ الْمُكَذِّبِيْنَ ﴿٣٧﴾

37. Na bila shaka Tulimwinua Mtume katika kila umati ya kwamba Mwabuduni Allah na muepukeni Mwovu. Basi yuko miongoni mwao ambaye Allah Amemwongoza, na yuko miongoni mwao ambaye upotevu umehakiki juu yake. Basi tembeeni katika ardhi na mwangalie ulikuwaje mwisho wa wakadhibishao.

اِنْ تَحْرِصْ عَلٰى هُدٰىهُمْ فَاِنَّ اللّٰهَ لَا يَهْدِيْ مَنْ يُّضِلُّ وَمَا لَهُمْ مِّنْ نّٰصِرِيْنَ ﴿٣٨﴾

38. Kama unayo tamaa ya kuongoka kwao, basi hakika Allah Hamwongozi yule anayepoteza (wengine). Nao hawana wasaidizi.

وَاَقْسَمُوْا بِاللّٰهِ جَهْدَ اَيْمَانِهِمْ ۙ لَا يَبْعَثُ اللّٰهُ مَنْ يَّمُوْتُ ؕ بَلٰى وَعْدًا عَلَيْهِ حَقًّا وَّلٰكِنَّ اَكْثَرَ النَّاسِ لَا يَعْلَمُوْنَ ﴿٣٩﴾ ۙ

39. Nao wakaapa kwa Allah kwa kiapo chao cha nguvu kwamba Allah Hatamfufua afaye. Naam, ni ahadi iliyolazimika Kwake, lakini watu wengi hawajui.

لِيُبَيِّنَ لَهُمُ الَّذِيْ يَخْتَلِفُوْنَ فِيْهِ وَلِيَعْلَمَ الَّذِيْنَ كَفَرُوْٓا اَنَّهُمْ كَانُوْا كٰذِبِيْنَ ﴿٤٠﴾

40. Ili kuwabainishia yale waliyohitilafiana kwayo na wajue waliokufuru ya kwamba wao walikuwa ni waongo.

41. Hakika kauli Yetu kwa kitu Tunachokitaka, Tunakiambia: Kuwa, basi kinakuwa.

إِنَّمَا قَوْلُنَا لِشَيْءٍ إِذَآ أَرَدْنَٰهُ أَن نَّقُولَ لَهُۥ كُن فَيَكُونُ ﴿٤١﴾

FUNGU 6

42. Na wale waliohama kwa ajili ya Allah baada ya kudhulumiwa, bila shaka Tutawakalisha katika dunia kwa wema; na ujira wa Akhera ni mkubwa zaidi; laiti wangalijua!

وَٱلَّذِينَ هَاجَرُوا۟ فِى ٱللَّهِ مِنۢ بَعْدِ مَا ظُلِمُوا۟ لَنُبَوِّئَنَّهُمْ فِى ٱلدُّنْيَا حَسَنَةً ۖ وَلَأَجْرُ ٱلْءَاخِرَةِ أَكْبَرُ ۚ لَوْ كَانُوا۟ يَعْلَمُونَ ﴿٤٢﴾

43. (Hao ni) wale wanaosubiri na wakamtegemea Mola wao.

ٱلَّذِينَ صَبَرُوا۟ وَعَلَىٰ رَبِّهِمْ يَتَوَكَّلُونَ ﴿٤٣﴾

44. Na hatukutuma kabla yako isipokuwa wanaume ambao Tuliwafunulia, basi waulizeni watu wenye kumbukumbu ikiwa ninyi hamjui.

وَمَآ أَرْسَلْنَا مِن قَبْلِكَ إِلَّا رِجَالًا نُّوحِىٓ إِلَيْهِمْ ۚ فَسْـَٔلُوٓا۟ أَهْلَ ٱلذِّكْرِ إِن كُنتُمْ لَا تَعْلَمُونَ ﴿٤٤﴾

45. (Tuliwatuma) kwa ishara zilizo wazi na misahafu. Na Tumekuteremshia ukumbusho ili uwafafanulie watu yale yaliyoteremshwa kwao, na ili wapate kutafakari.

بِٱلْبَيِّنَٰتِ وَٱلزُّبُرِ ۗ وَأَنزَلْنَآ إِلَيْكَ ٱلذِّكْرَ لِتُبَيِّنَ لِلنَّاسِ مَا نُزِّلَ إِلَيْهِمْ وَلَعَلَّهُمْ يَتَفَكَّرُونَ ﴿٤٥﴾

46. Je, wako salama wale waliofanya hila mbaya ya kwamba Allah Hatawadidimiza katika ardhi au kuwafikia adhabu kutoka wasipopajua?

أَفَأَمِنَ ٱلَّذِينَ مَكَرُوا۟ ٱلسَّيِّـَٔاتِ أَن يَخْسِفَ ٱللَّهُ بِهِمُ ٱلْأَرْضَ أَوْ يَأْتِيَهُمُ ٱلْعَذَابُ مِنْ حَيْثُ لَا يَشْعُرُونَ ﴿٤٦﴾

47. Au Hatawakamata katika kwenda kwao huko na huko, kisha hawataweza kuponyoka?

أَوْ يَأْخُذَهُمْ فِى تَقَلُّبِهِمْ فَمَا هُم بِمُعْجِزِينَ ﴿٤٧﴾

48. Au hatawakamata kwa kuwaadhibu kidogo kidogo? Hakika Mola wenu ni Mpole, Mrehemevu.

أَوْ يَأْخُذَهُمْ عَلَىٰ تَخَوُّفٍ ۖ فَإِنَّ رَبَّكُمْ لَرَءُوفٌ رَّحِيمٌ ﴿٤٨﴾

Aya 45. *Adh-Dhikr,* neno hili limetafsiriwa "mauidha," na pia lina maana hizi: (1) Ukumbusho, (2) kitu kuwa katika akili na kisisahauliwe; (3) utukufu, na heshima; (4) Kitabu chenye maelezo ya dini na kanuni za dini; (5) usemi ulio imara na wenye nguvu (Lane). Sifa zote hizi zinapatikana katika Qur'an. Kitabu hiki (a) kinamsaidia mtu kumkumbuka Mungu; (b) kinamsifu na kumtukuza Mungu; (c) wanaotenda sawa na mafundisho yake hupata heshima na utukufu; (d) kina maelezo ya dini ya Kiislamu; (e) kina nguvu na ni imara wala mafundisho yake hayana shaka, yamenyoka.

49. Je, hawaoni kila kitu Alichoumba Allah, vivuli vyake vinazunguka kutoka kulia na kushoto vikimsujudia Allah, hali wamedhalilika?

اَوَلَمۡ يَرَوۡا اِلٰى مَا خَلَقَ اللّٰهُ مِنۡ شَىۡءٍ يَّتَفَيَّؤُا ظِلٰلُهٗ عَنِ الۡيَمِيۡنِ وَالشَّمَآئِلِ سُجَّدًا لِّلّٰهِ وَهُمۡ دٰخِرُوۡنَ ﴿۴۹﴾

50. Na vinamsujudia Allah vilivyomo mbinguni na vilivyomo ardhini katika wanyama na Malaika pia, nao hawatakabari.

وَلِلّٰهِ يَسۡجُدُ مَا فِى السَّمٰوٰتِ وَمَا فِى الۡاَرۡضِ مِنۡ دَآبَّةٍ وَّالۡمَلٰٓئِكَةُ وَهُمۡ لَا يَسۡتَكۡبِرُوۡنَ ﴿۵۰﴾

51. Wanamwogopa Mola wao Aliye juu yao, na wanatenda wanayoamrishwa.

يَخَافُوۡنَ رَبَّهُمۡ مِّنۡ فَوۡقِهِمۡ وَيَفۡعَلُوۡنَ مَا يُؤۡمَرُوۡنَ ﴿۵۱﴾ ۩

FUNGU 7

52. Na Allah Amesema: Msishike waungu wawili; hakika Yeye ni Mungu Mmoja tu: basi Niogopeni Mimi tu.

وَقَالَ اللّٰهُ لَا تَتَّخِذُوۡۤا اِلٰهَيۡنِ اثۡنَيۡنِ‌ۚ اِنَّمَا هُوَ اِلٰهٌ وَّاحِدٌ‌ۚ فَاِيَّاىَ فَارۡهَبُوۡنِ ﴿۵۲﴾

53. Na ni Vyake vyote vilivyomo mbinguni na ardhini, na utii unawajibika Kwake tu. Basi je mtamwogopa mwingine ye yote asiyekuwa Allah?

وَلَهٗ مَا فِى السَّمٰوٰتِ وَالۡاَرۡضِ وَلَهُ الدِّيۡنُ وَاصِبًا‌ؕ اَفَغَيۡرَ اللّٰهِ تَتَّقُوۡنَ ﴿۵۳﴾

54. Na neema yo yote mliyonayo imetoka kwa Allah. Kisha inapowaguseni dhara, basi Yeye mnamlilia.

وَمَا بِكُمۡ مِّنۡ نِّعۡمَةٍ فَمِنَ اللّٰهِ ثُمَّ اِذَا مَسَّكُمُ الضُّرُّ فَاِلَيۡهِ تَجۡـَٔرُوۡنَ ﴿۵۴﴾

55. Kisha Anapowaondoleeni dhara, mara kundi moja miongoni mwenu linamshirikisha Mola wao;

ثُمَّ اِذَا كَشَفَ الضُّرَّ عَنۡكُمۡ اِذَا فَرِيۡقٌ مِّنۡكُمۡ بِرَبِّهِمۡ يُشۡرِكُوۡنَ ﴿۵۵﴾

56. Ili wavikatae Tulivyowapa. Basi jifaidisheni kidogo, nanyi hivi karibuni mtajua.

لِيَكۡفُرُوۡا بِمَاۤ اٰتَيۡنٰهُمۡ‌ؕ فَتَمَتَّعُوۡا‌ۖ فَسَوۡفَ تَعۡلَمُوۡنَ ﴿۵۶﴾

57. Na wanawawekea (waungu wao) wasiowafahamu sehemu katika vile Tulivyowapa. Kwa haki ya Allah, bila shaka ninyi mtaulizwa juu ya yale mliyokuwa mkiyatunga.

وَيَجۡعَلُوۡنَ لِمَا لَا يَعۡلَمُوۡنَ نَصِيۡبًا مِّمَّا رَزَقۡنٰهُمۡ‌ؕ تَاللّٰهِ لَتُسۡـَٔلُنَّ عَمَّا كُنۡتُمۡ تَفۡتَرُوۡنَ ﴿۵۷﴾

58. Na wanamwekea Allah mabinti, Subhana! hali wao hupata wanavyovitaka.

وَيَجْعَلُوْنَ لِلّٰهِ الْبَنٰتِ سُبْحٰنَهٗ ۙ وَلَهُمْ مَّا يَشْتَهُوْنَ ﴿٥٨﴾

59. Na mmoja wao anapopewa habari ya (kuzaliwa mtoto) wa kike, uso wake huwa mweusi, naye anazuia sikitiko.

وَاِذَا بُشِّرَ اَحَدُهُمْ بِالْاُنْثٰى ظَلَّ وَجْهُهٗ مُسْوَدًّا وَّهُوَ كَظِيْمٌ ۚ ﴿٥٩﴾

60. Hujificha na watu kwa sababu ya ubaya alioambiwa. Je, amchukue juu ya fedheha au amfukie udongoni? Sikilizeni! ni mabaya wanayoyahukumu.

يَتَوَارٰى مِنَ الْقَوْمِ مِنْ سُوْٓءِ مَا بُشِّرَ بِهٖ ؕ اَيُمْسِكُهٗ عَلٰى هُوْنٍ اَمْ يَدُسُّهٗ فِى التُّرَابِ ؕ اَلَا سَآءَ مَا يَحْكُمُوْنَ ﴿٦٠﴾

61. Methali mbaya kuliko zote inawahusu wale wasioamini Akhera; ambapo sifa iliyo tukufu kuliko zote ni ya Allah, naye ni Mwenye ushindi kamili, Mwenye hekima.

لِلَّذِيْنَ لَا يُؤْمِنُوْنَ بِالْاٰخِرَةِ مَثَلُ السَّوْءِ ۚ وَلِلّٰهِ الْمَثَلُ الْاَعْلٰى ؕ وَهُوَ الْعَزِيْزُ الْحَكِيْمُ ﴿٦١﴾ ع ۱۳

FUNGU 8

62. Na lau Allah Angaliwakamata watu kwa sababu ya dhuluma yao, Asingaliacha hata mnyama mmoja; lakini Anawaahirisha mpaka muda uliowekwa; na unapofika muda wao, hawawezi kuikawiza saa moja wala hawawezi kuitanguliza.

وَلَوْ يُؤَاخِذُ اللّٰهُ النَّاسَ بِظُلْمِهِمْ مَّا تَرَكَ عَلَيْهَا مِنْ دَآبَّةٍ وَّلٰكِنْ يُّؤَخِّرُهُمْ اِلٰٓى اَجَلٍ مُّسَمًّى ۚ فَاِذَا جَآءَ اَجَلُهُمْ لَا يَسْتَاْخِرُوْنَ سَاعَةً وَّلَا يَسْتَقْدِمُوْنَ ﴿٦٢﴾

Aya 58. *Na wanamwekea Allah mabinti.* Waarabu wa zamani waliamini Malaika kuwa ni binti za Mungu, na wenyewe hawakutaka kuwa na mabinti. Basi wanalaumiwa kusema juu ya Allah ambayo hawataki kwa ajili ya nafsi zao. Wakristo pia wanamwita Yesu mwana wa Mungu, tena wanasema Mungu alipenda mwanawe auawe. Wanafanana na wale washirikina waliompa Mungu sifa ambazo wao wenyewe hawakupenda kuzipewa. Wakristo wasingependa kuwatoa wana wao wauawe kwa ajili ya makosa ya watu wengine; bali wanafikiri kuwa Mungu ana mwana, na alipenda mwanawe huyo auawe kwa ajili ya makosa ya watu wengine!

Kwa kuwa mambo mengi ya Ukristo yamechukuliwa kutoka upagani, Wakristo pia wanawafananisha Malaika na wanawake wenye mbawa. Wakatoliki wa siku hizi wamepita kiasi katika upagani: wamepiga picha ya Mungu kama mtu mzee, mwenye ndevu!

Aya 60. Katika Aya hizi Qur'an inalaumu tabia ya baadhi ya Waarabu ambao waliwadhalilisha wanawake hata wakafika kuwazika hai baadhi ya binti zao. Dini ya Kiislamu imetia mkazo sana juu ya heshima ya wanawake na kuwatendea wema.

وَيَجْعَلُوْنَ لِلّٰهِ مَا يَكْرَهُوْنَ وَتَصِفُ
اَلْسِنَتُهُمُ الْكَذِبَ اَنَّ لَهُمُ الْحُسْنٰى ؕ لَا
جَرَمَ اَنَّ لَهُمُ النَّارَ وَاَنَّهُمْ مُّفْرَطُوْنَ ﴿٦٢﴾

63. Na wanampa Allah wanavyovichukia, na ndimi zao zinasema uwongo kwamba wao watapata mema. Bila shaka wamewekewa Moto, nao wataachwa (mumo humo).

تَاللّٰهِ لَقَدْ اَرْسَلْنَاۤ اِلٰۤى اُمَمٍ مِّنْ قَبْلِكَ
فَزَيَّنَ لَهُمُ الشَّيْطٰنُ اَعْمَالَهُمْ فَهُوَ
وَلِيُّهُمُ الْيَوْمَ وَلَهُمْ عَذَابٌ اَلِيْمٌ ﴿٦٣﴾

64. Kwa haki ya Allah, Sisi Tulituma (Mitume) kwa watu wa kabla yako; lakini Shetani akawapambia vitendo vyao, kwa hiyo leo yeye ni rafiki yao; nao watapata adhabu iumizayo.

وَمَاۤ اَنْزَلْنَا عَلَيْكَ الْكِتٰبَ اِلَّا لِتُبَيِّنَ لَهُمُ
الَّذِى اخْتَلَفُوْا فِيْهِ ۙ وَهُدًى وَّرَحْمَةً
لِّقَوْمٍ يُّؤْمِنُوْنَ ﴿٦٤﴾

65. Na Hatukukuteremshia Kitabu isipokuwa uwabainishie yale ambayo wanahitilafiana, na (pia kiwe) mwongozo na rehema kwa watu wanaoamini.

وَاللّٰهُ اَنْزَلَ مِنَ السَّمَآءِ مَآءً فَاَحْيَا بِهِ
الْاَرْضَ بَعْدَ مَوْتِهَا ؕ اِنَّ فِىْ ذٰلِكَ لَاٰيَةً
لِّقَوْمٍ يَّسْمَعُوْنَ ﴿٦٥﴾ ع ١٤

66. Na Allah Ameteremsha maji kutoka mbinguni na kwayo Akaihuisha ardhi baada ya kufa kwake. Kwa hakika katika hayo imo Ishara kwa watu wasikiao.

FUNGU 9

وَاِنَّ لَكُمْ فِى الْاَنْعَامِ لَعِبْرَةً ؕ نُسْقِيْكُمْ
مِّمَّا فِىْ بُطُوْنِهٖ مِنْۢ بَيْنِ فَرْثٍ وَّدَمٍ
لَّبَنًا خَالِصًا سَآئِغًا لِّلشّٰرِبِيْنَ ﴿٦٦﴾

67. Na bila shaka katika wanyama liko fundisho kwa ajili yenu. Tunawanywesheni katika vile vilivyomo matumboni mwao, baina ya mavi na damu, maziwa halisi, mazuri kwa wanywao.

وَمِنْ ثَمَرٰتِ النَّخِيْلِ وَالْاَعْنَابِ
تَتَّخِذُوْنَ مِنْهُ سَكَرًا وَّرِزْقًا حَسَنًا ؕ اِنَّ فِىْ
ذٰلِكَ لَاٰيَةً لِّقَوْمٍ يَّعْقِلُوْنَ ﴿٦٧﴾

68. Na katika matunda ya mitende na mizabibu ambayo mnaitengenezea kileo na riziki nzuri. Hakika katika hayo imo Ishara kwa watu watumiao akili.

Aya 68. *Ambayo mnaitengeneza kileo.*

Katika Aya 67 Allah ameeleza tendo Lake linalostaajabisha mno; jinsi alivyotoa mifereji ya maziwa safi toka katika mavi na damu. Katika Aya hii Allah ameonyesha ujinga wa baadhi ya watu wanaopewa matunda mazuri na matamu nao wakayageuza kuwa kileo.

Mungu anataka kuvunja dalili ya wale ambao wakiisha kupata elimu kidogo wanajivuna na kusema, sisi hatuna haja ya mwongozo utokao kwa Mungu, tutatunga sisi wenyewe sheria ya kutufaa. Wanajibiwa hivi, mtawezaje kutunga sheria hali ubovu wa akili yenu umekwisha dhihirika, maana mlipewa matunda mazuri nanyi mliyaharibu mkatengeneza kwayo mvinyo. Mungu ndiye anayeweza kuwaongozeni ambaye akili yake na uwezo Wake vimeonekana katika kutengeneza maziwa yaliyo safi na halisi.

وَاَوْحٰى رَبُّكَ اِلَى النَّحْلِ اَنِ اتَّخِذِىْ مِنَ الْجِبَالِ بُيُوْتًا وَّمِنَ الشَّجَرِ وَمِمَّا يَعْرِشُوْنَ ﴿٦٩﴾

69. Na Mola wako Akamfunulia nyuki ya kwamba utengeneze majumba katika milima na katika miti na katika yale wanayojenga (watu).

ثُمَّ كُلِىْ مِنْ كُلِّ الثَّمَرٰتِ فَاسْلُكِىْ سُبُلَ رَبِّكِ ذُلُلًا ؕ يَخْرُجُ مِنْۢ بُطُوْنِهَا شَرَابٌ مُّخْتَلِفٌ اَلْوَانُهٗ فِيْهِ شِفَآءٌ لِّلنَّاسِ ؕ اِنَّ فِىْ ذٰلِكَ لَاٰيَةً لِّقَوْمٍ يَّتَفَكَّرُوْنَ ﴿٧٠﴾

70. Kisha kula kila aina ya matunda na utembee kwa unyenyekevu katika njia za Mola wako. Kinatoka katika matumbo yao kinywaji chenye rangi mbalimbali. Ndani yake kuna ponyo kwa ajili ya binadamu. Hakika katika hayo iko ishara kwa watu wenye kutafakari.

وَاللّٰهُ خَلَقَكُمْ ثُمَّ يَتَوَفّٰكُمْ ۙ وَمِنْكُمْ مَّنْ يُّرَدُّ اِلٰٓى اَرْذَلِ الْعُمُرِ لِكَيْ لَا يَعْلَمَ بَعْدَ عِلْمٍ شَيْـًٔا ؕ اِنَّ اللّٰهَ عَلِيْمٌ قَدِيْرٌ ﴿٧١﴾ ع ١٥

71. Na Allah Huwaumbeni, kisha Huwafisheni; na miongoni mwenu yuko anayerudishwa katika umri wa udhaifu ndipo anakuwa hajui chochote baada ya (kuwa na) ujuzi. Kwa hakika Allah ni Mjuzi wa yote, Mweza.

FUNGU 10

وَاللّٰهُ فَضَّلَ بَعْضَكُمْ عَلٰى بَعْضٍ فِى الرِّزْقِ ۚ فَمَا الَّذِيْنَ فُضِّلُوْا بِرَآدِّىْ رِزْقِهِمْ عَلٰى مَا مَلَكَتْ اَيْمَانُهُمْ فَهُمْ فِيْهِ سَوَآءٌ ؕ اَفَبِنِعْمَةِ اللّٰهِ يَجْحَدُوْنَ ﴿٧٢﴾

72. Na Allah Amewafadhilini baadhi yenu kuliko wengine katika riziki. Lakini wale waliofadhiliwa hawarudishi riziki zao kwa wale iliowatamalaki mikono yao ya kuume ili wawe sawa katika (riziki) hii. Basi je, wanazikataa neema za Allah?

Padre Dale, katika Tafsiri yake ukurasa 555, anasema, baadhi ya Waislamu wanataja Aya hii kuwa dalili ya kuhalalisha pombe. Neno hili limetushangaza sana. Kila mtu anayefahamu Kiswahili na asome tafsiri ya Aya hii kisha aseme kama pombe imeruhusiwa humo. Padre huyo ameandika tafsiri ya Aya hii kama hivi: "Katika miti hiyo mnajipatia divai na riziki nzuri" (uk. 247). Hata tukifuata tafsiri hiyo haionekani kama pombe imeruhusiwa.

Aya 69. Somo lililopo hapa ni kuwa ikiwa hata viumbe kama nyuki Mungu amevifunulia wahyi ili vipate kuendesha kazi sawa na makusudio yao, je, siyo zaidi sana kwa mwanadamu ambaye maendeleo yake hayana kikomo ya kwamba asiachwe bila kuongozwa na ufunuo wa Allah?

وَاللّٰهُ جَعَلَ لَكُمْ مِّنْ اَنْفُسِكُمْ اَزْوَاجًا وَّجَعَلَ لَكُمْ مِّنْ اَزْوَاجِكُمْ بَنِيْنَ وَحَفَدَةً وَّرَزَقَكُمْ مِّنَ الطَّيِّبٰتِ ؕ اَفَبِالْبَاطِلِ يُؤْمِنُوْنَ وَبِنِعْمَتِ اللّٰهِ هُمْ يَكْفُرُوْنَ ﴿۷۲﴾

73. Na Allah Amewajaalieni wake katika jinsi yenu, na akawajaalieni kutoka kwa wake zenu watoto na wajukuu, na kuwaruzukuni katika vitu vizuri. Basi je, wanaamini batili na kuzikataa neema za Allah?

وَيَعْبُدُوْنَ مِنْ دُوْنِ اللّٰهِ مَا لَا يَمْلِكُ لَهُمْ رِزْقًا مِّنَ السَّمٰوٰتِ وَالْاَرْضِ شَيْـًٔا وَّلَا يَسْتَطِيْعُوْنَ ﴿۷۳﴾

74. Na wanawaabudu kinyume cha Allah wasiowamilikia riziki hata kidogo kutoka mbinguni na ardhini, wala hawana uwezo.

فَلَا تَضْرِبُوْا لِلّٰهِ الْاَمْثَالَ ؕ اِنَّ اللّٰهَ يَعْلَمُ وَاَنْتُمْ لَا تَعْلَمُوْنَ ﴿۷۴﴾

75. Basi msimpigie Allah mifano. Hakika Allah Anajua na ninyi hamjui.

ضَرَبَ اللّٰهُ مَثَلًا عَبْدًا مَّمْلُوْكًا لَّا يَقْدِرُ عَلٰى شَيْءٍ وَّمَنْ رَّزَقْنٰهُ مِنَّا رِزْقًا حَسَنًا فَهُوَ يُنْفِقُ مِنْهُ سِرًّا وَّجَهْرًا ؕ هَلْ يَسْتَوٗنَ ؕ اَلْحَمْدُ لِلّٰهِ ؕ بَلْ اَكْثَرُهُمْ لَا يَعْلَمُوْنَ ﴿۷۵﴾

76. Allah Anapiga mfano wa mtumwa anayemilikiwa; asiyeweza cho chote; na (mwingine) Tuliyemruzuku kutoka Kwetu riziki njema, naye anatoa katika hiyo kwa siri na dhahiri. Je, wako sawa? Sifa zote njema ni za Allah! lakini wengi wao hawajui.

وَضَرَبَ اللّٰهُ مَثَلًا رَّجُلَيْنِ اَحَدُهُمَآ اَبْكَمُ لَا يَقْدِرُ عَلٰى شَيْءٍ وَّهُوَ كَلٌّ عَلٰى مَوْلٰىهُ ۙ اَيْنَمَا يُوَجِّهْهُّ لَا يَاْتِ بِخَيْرٍ ؕ هَلْ يَسْتَوِيْ هُوَ ۙ وَمَنْ يَّاْمُرُ بِالْعَدْلِ ۙ وَهُوَ عَلٰى صِرَاطٍ مُّسْتَقِيْمٍ ﴿۷۶﴾ ع

77. Na Allah Anapiga mfano wa watu wawili: mmoja wao ni bubu, hawezi cho chote, naye ni mzigo juu ya bwana wake, po pote amtumapo haleti heri. Je, huyu anaweza kuwa sawa na yule anayeamuru kwa uadilifu naye yu juu ya njia iliyonyooka?

FUNGU 11

وَلِلّٰهِ غَيْبُ السَّمٰوٰتِ وَالْاَرْضِ ؕ وَمَآ اَمْرُ السَّاعَةِ اِلَّا كَلَمْحِ الْبَصَرِ اَوْ هُوَ اَقْرَبُ ؕ اِنَّ اللّٰهَ عَلٰى كُلِّ شَيْءٍ قَدِيْرٌ ﴿۷۷﴾

78. Na ni Vya Allah visivyoonekana vya mbingu na ardhi; na jambo la (kufika) saa (ile) ni kama tu kupepesa jicho au ni karibu zaidi. Hakika Allah ni Mweza wa kila kitu.

وَاللّٰهُ اَخْرَجَكُمْ مِّنْۢ بُطُوْنِ اُمَّهٰتِكُمْ
لَا تَعْلَمُوْنَ شَيْـًٔا ۙ وَّ جَعَلَ لَكُمُ السَّمْعَ
وَالْاَبْصَارَ وَالْاَفْـِٕدَةَ ۙ لَعَلَّكُمْ تَشْكُرُوْنَ ﴿۷۸﴾

79. Na Allah Amewatoeni matumboni mwa mama zenu hali hamjui cho chote, na Amewajaalieni masikio na macho na mioyo ili mpate kushukuru.

اَلَمْ يَرَوْا اِلَى الطَّيْرِ مُسَخَّرٰتٍ فِيْ جَوِّ
السَّمَآءِ ؕ مَا يُمْسِكُهُنَّ اِلَّا اللّٰهُ ؕ اِنَّ فِيْ
ذٰلِكَ لَاٰيٰتٍ لِّقَوْمٍ يُّؤْمِنُوْنَ ﴿۷۹﴾

80. Je hawaoni ndege walioti-ishwa katika anga la mbingu? Hakuna Anayewashikilia huko angani isipokuwa Allah. Bila shaka katika hayo zimo ishara kwa watu wanaoamini.

وَاللّٰهُ جَعَلَ لَكُمْ مِّنْۢ بُيُوْتِكُمْ سَكَنًا
وَّجَعَلَ لَكُمْ مِّنْ جُلُوْدِ الْاَنْعَامِ بُيُوْتًا
تَسْتَخِفُّوْنَهَا يَوْمَ ظَعْنِكُمْ وَ يَوْمَ
اِقَامَتِكُمْ ۙ وَمِنْ اَصْوَافِهَا وَاَوْبَارِهَا
وَاَشْعَارِهَاۤ اَثَاثًا وَّ مَتَاعًا اِلٰى حِيْنٍ ﴿۸۰﴾

81. Na Allah Amewajaalieni majumba yenu yawe makao (yenu), na (pia) Amewajaalieni majumba katika ngozi za wanyama, mnazoziona nyepesi wakati wa safari yenu, na wakati wa kuweka kwenu kituo; na katika sufu zao, na manyoya yao, na nywele zao, (mnatengeneza) vyombo na vifaa vya kutumia kwa muda.

وَاللّٰهُ جَعَلَ لَكُمْ مِّمَّا خَلَقَ ظِلٰلًا وَّ جَعَلَ
لَكُمْ مِّنَ الْجِبَالِ اَكْنَانًا وَّ جَعَلَ لَكُمْ
سَرَابِيْلَ تَقِيْكُمُ الْحَرَّ وَسَرَابِيْلَ
تَقِيْكُمْ بَاْسَكُمْ ؕ كَذٰلِكَ يُتِمُّ نِعْمَتَهٗ
عَلَيْكُمْ لَعَلَّكُمْ تُسْلِمُوْنَ ﴿۸۱﴾

82. Na Allah Amewafanyieni katika vile Alivyoviumba, vitu vitiavyo kivuli; na Amewafanyieni makimbilio katika milima, na Amewafanyieni kanzu zinazowakingeni na joto, na dereya zinazowakingeni katika vita zenu. Hivi ndivyo Huwatimizieni neema Zake ili mpate kutii.

فَاِنْ تَوَلَّوْا فَاِنَّمَا عَلَيْكَ الْبَلٰغُ الْمُبِيْنُ ﴿۸۲﴾

83. Lakini wakikengeuka, basi si juu yako ila kufikisha (ujumbe) waziwazi.

يَعْرِفُوْنَ نِعْمَتَ اللّٰهِ ثُمَّ يُنْكِرُوْنَهَا
وَاَكْثَرُهُمُ الْكٰفِرُوْنَ ﴿۸۳﴾ ع ۱۱

84. Wanazifahamu neema za Allah kisha wanazikataa, na wengi wao ni makafiri.

FUNGU 12

وَيَوْمَ نَبْعَثُ مِنْ كُلِّ اُمَّةٍ شَهِيْدًا ثُمَّ لَا يُؤْذَنُ لِلَّذِيْنَ كَفَرُوْا وَلَا هُمْ يُسْتَعْتَبُوْنَ ﴿٨٥﴾

85. Na siku Tutakayomwinua shahidi katika kila umati, kisha haitaruhusiwa kwa waliokufuru (kujisahihisha), wala hawatakubaliwa udhuru (wao).

وَاِذَا رَاَ الَّذِيْنَ ظَلَمُوا الْعَذَابَ فَلَا يُخَفَّفُ عَنْهُمْ وَلَا هُمْ يُنْظَرُوْنَ ﴿٨٦﴾

86. Na wale waliodhulumu watakapoiona adhabu, basi hawatapu-nguziwa wala hawatapewa muhula.

وَاِذَا رَاَ الَّذِيْنَ اَشْرَكُوْا شُرَكَآءَهُمْ قَالُوْا رَبَّنَا هٰٓؤُلَآءِ شُرَكَآؤُنَا الَّذِيْنَ كُنَّا نَدْعُوْا مِنْ دُوْنِكَ ۚ فَاَلْقَوْا اِلَيْهِمُ الْقَوْلَ اِنَّكُمْ لَكٰذِبُوْنَ ﴿٨٧﴾ ع

87. Na walioshirikisha watakapowaona washirika wao, watasema: Mola wetu, hao ndio washirika wetu ambao tulikuwa tukiwaita badala Yako. Ndipo watawatupia neno: Hakika ninyi ni waongo.

وَاَلْقَوْا اِلَى اللّٰهِ يَوْمَئِذِ السَّلَمَ وَضَلَّ عَنْهُمْ مَّا كَانُوْا يَفْتَرُوْنَ ﴿٨٨﴾

88. Na siku hiyo watajitoa kutii mbele ya Allah, na yatawapotea waliyokuwa wakiyatunga.

اَلَّذِيْنَ كَفَرُوْا وَصَدُّوْا عَنْ سَبِيْلِ اللّٰهِ زِدْنٰهُمْ عَذَابًا فَوْقَ الْعَذَابِ بِمَا كَانُوْا يُفْسِدُوْنَ ﴿٨٩﴾

89. (Ama) wale waliokufuru na kuwazuilia (watu) njia ya Allah, Tutawazidishia adhabu juu ya adhabu kwa sababu walikuwa wakifisidi.

وَيَوْمَ نَبْعَثُ فِيْ كُلِّ اُمَّةٍ شَهِيْدًا عَلَيْهِمْ مِّنْ اَنْفُسِهِمْ وَجِئْنَا بِكَ شَهِيْدًا عَلٰى هٰٓؤُلَآءِ ؕ وَنَزَّلْنَا عَلَيْكَ الْكِتٰبَ تِبْيَانًا لِّكُلِّ شَيْءٍ وَّهُدًى وَّرَحْمَةً وَّبُشْرٰى لِلْمُسْلِمِيْنَ ﴿٨٩﴾ ع ١٨

90. Na siku Tutakayomwinua shahidi katika kila umati juu yao kutoka miongoni mwao, na wewe Tutakuleta uwe shahidi juu ya hawa. Na Tumekuteremshia Kitabu kielezacho kila kitu, na mwongozo, na rehema, na habari za furaha kwa wajisalimishao.

FUNGU 13

اِنَّ اللّٰهَ يَاْمُرُ بِالْعَدْلِ وَالْاِحْسَانِ وَاِيْتَآئِ ذِي الْقُرْبٰى وَيَنْهٰى عَنِ الْفَحْشَآءِ وَالْمُنْكَرِ وَالْبَغْيِ ۚ يَعِظُكُمْ لَعَلَّكُمْ تَذَكَّرُوْنَ ﴿٩٠﴾

91. Kwa hakika Allah Anaamuru uadilifu, na hisani, na kuwapa (watu kama uwapavyo) ndugu; na Anakataza upujufu, na uovu, na uasi. Anawanasihini ili mpate kufahamu.

Aya 91. Katika Aya hii wema unaonyeshwa kuwa na madaraja matatu, na kadhalika ubaya una madaraja matatu. Daraja ya kwanza ya wema inaitwa *'adl,* yaani uadilifu, ya kwamba yampasa

92. Na timizeni ahadi ya Allah mnapoahidi; wala msivunje viapo baada ya kuvithibitisha, hali mmekwisha Mfanya Allah kuwa Mdhamini wenu. Hakika Allah Anayajua mnayoyafanya.

وَاَوْفُوْا بِعَهْدِ اللّٰهِ اِذَا عٰهَدْتُّمْ وَلَا تَنْقُضُوا
الْاَيْمَانَ بَعْدَ تَوْكِيْدِهَا وَقَدْ جَعَلْتُمُ اللّٰهَ
عَلَيْكُمْ كَفِيْلًا ؕ اِنَّ اللّٰهَ يَعْلَمُ مَا
تَفْعَلُوْنَ ﴿٩٢﴾

93. Wala msiwe kama yule mwanamke aliyekata uzi wake vipande-vipande baada ya (kuusokota) kuwa mgumu. Mnavifanya viapo vyenu njia ya kudanganyana kati yenu ili lisije kundi moja la watu kuwa na nguvu zaidi

وَلَا تَكُوْنُوْا كَالَّتِيْ نَقَضَتْ غَزْلَهَا مِنْۢ
بَعْدِ قُوَّةٍ اَنْكَاثًا ؕ تَتَّخِذُوْنَ اَيْمَانَكُمْ
دَخَلًۢا بَيْنَكُمْ اَنْ تَكُوْنَ اُمَّةٌ هِيَ اَرْبٰى

---

mtu awatendee wenziwe kama anavyotendewa na wao, na yampasa alipe wema anaotendewa kwa wema kiasi kile kile. Pia yampasa awafikirie wengine kwa uadilifu, yaani awafikirie kama apendavyo wao wamfikirie yeye. Haimpasi kulipa mema kwa mabaya wala kutazamia alipwe mema kwa uovu. Maovu hayamo katika maana ya *'adl. 'Adl* inamruhusu mtu kumpa adhabu mkosaji sawa na kosa lake; lakini haimruhusu mtu kumwadhibu mkosaji kwa kufanya kitendo kiovu kama kile kilichofanywa na mkosaji, maana uovu ni sumu na alaye sumu kwa kumwadhibu mtu aliyekula sumu amefanya upumbavu.

Daraja ya pili ya wema inaitwa *ihsaan,* yaani kutenda wema zaidi kuliko uliotendewa, na kuwasamehe wenye kukukosea isipokuwa katika mambo ambayo kusamehe wenye kukosa kunaweza kuzidisha machafuko.

Daraja ya tatu ya wema iliyo juu ya hiyo inaitwa *iitai dhil qurbaa,* yaani kutenda wema kama vile wazazi wamtendeavyo wema mtoto wao, hawamtendei wema kwa kuwa naye alipata kuwatendea wema na sasa wamlipe, wala hawamtendei wema kwa kutazamia kuwa atawalipa wema wao, hasha.

Na daraja ya kwanza ya uovu inaitwa *Fahshaa,* neno ambalo likitumiwa pamoja na *munkar* maana yake inakuwa uovu wa siri usiojionyesha, kama vile mawazo mabaya yatokayo katika moyo mbaya, na mashawishi ya urafiki mbaya na mafundisho mabaya. Kama hayakung'olewa mapema, na yakiachwa kutia mizizi, mwishoni yanashinda, na misingi ya kwanza ya uovu inasimamishwa.

Kisha inaanza daraja ya pili ya uovu, inayoitwa *munkar* ambayo inadhuru matendo na tabia ya mwanadamu. Watu wengine wanachukizwa na tabia ya namna hiyo na wanaisema vibaya, lakini hapo pote hali hiyo inaishia katika matendo yanayomdhuru mtu mmoja pekee, kwa mfano maneno ya upuuzi, uwongo na mengineyo.

Na anaposhindwa kuuangalia mwenendo wake vyema, hapo anashuka moja kwa moja katika daraja la tatu la uovu linaloitwa *baghyu,* yaani uovu unaodhuru watu wengine na kuzivunja dhahiri sheria za tabia njema, na mtu anakuwa anapendezwa na uovu na anajivuna nao, na kumlaumu au kumwonya kunakuwa hakufai kitu.

مِنْ اُمَّةٍ ؕ اِنَّمَا يَبْلُوْكُمُ اللّٰهُ بِهٖ ؕ وَلَيُبَيِّنَنَّ لَكُمْ يَوْمَ الْقِيٰمَةِ مَا كُنْتُمْ فِيْهِ تَخْتَلِفُوْنَ ﴿٩٣﴾

kuliko kundi la watu wengine. Hakika Allah Atawajaribuni kwa njia hiyo, na bila shaka Atawabainishieni siku ya Kiyama mliyokuwa mkihitilafiana.

وَلَوْ شَآءَ اللّٰهُ لَجَعَلَكُمْ اُمَّةً وَّاحِدَةً وَّلٰكِنْ يُّضِلُّ مَنْ يَّشَآءُ وَيَهْدِىْ مَنْ يَّشَآءُ ؕ وَلَتُسْـَٔلُنَّ عَمَّا كُنْتُمْ تَعْمَلُوْنَ ﴿٩٤﴾

94. Na Allah Angalitaka, kwa yakini angaliwafanyeni kundi moja; lakini anayetaka (upotevu) Anampoteza, na anayetaka (mwongozo) Anamwongoza; na hakika mtaulizwa juu ya yale mliyokuwa mkifanya.

وَلَا تَتَّخِذُوْٓا اَيْمَانَكُمْ دَخَلًاۢ بَيْنَكُمْ فَتَزِلَّ قَدَمٌۢ بَعْدَ ثُبُوْتِهَا وَتَذُوْقُوا السُّوْٓءَ بِمَا صَدَدْتُّمْ عَنْ سَبِيْلِ اللّٰهِ ۚ وَلَكُمْ عَذَابٌ عَظِيْمٌ ﴿٩٥﴾

95. Wala msivifanye viapo vyenu njia ya kudanganyana baina yenu, isije mguu ukateleza baada ya kuuimarisha, na mkayaonja (malipo ya) maovu kwa sababu ya kuzuilia kwenu njia ya Allah, na mkapata adhabu kubwa.

وَلَا تَشْتَرُوْا بِعَهْدِ اللّٰهِ ثَمَنًا قَلِيْلًا ؕ اِنَّمَا عِنْدَ اللّٰهِ هُوَ خَيْرٌ لَّكُمْ اِنْ كُنْتُمْ تَعْلَمُوْنَ ﴿٩٦﴾

96. Wala msiuze ahadi ya Allah kwa thamani ndogo. Kilichoko kwa Allah ndicho bora kwenu ikiwa mnajua.

مَا عِنْدَكُمْ يَنْفَدُ ۚ وَمَا عِنْدَ اللّٰهِ بَاقٍ ؕ وَلَنَجْزِيَنَّ الَّذِيْنَ صَبَرُوْٓا اَجْرَهُمْ بِاَحْسَنِ مَا كَانُوْا يَعْمَلُوْنَ ﴿٩٧﴾

97. Mlivyo navyo vitakwisha na vilivyoko kwa Allah ndivyo vibakiavyo; na kwa yakini Sisi Tutawapa waliosubiri ujira wao sawa na matendo mazuri waliyokuwa wakiyatenda.

مَنْ عَمِلَ صَالِحًا مِّنْ ذَكَرٍ اَوْ اُنْثٰى وَهُوَ مُؤْمِنٌ فَلَنُحْيِيَنَّهٗ حَيٰوةً طَيِّبَةً ۚ وَلَنَجْزِيَنَّهُمْ اَجْرَهُمْ بِاَحْسَنِ مَا كَانُوْا يَعْمَلُوْنَ ﴿٩٨﴾

98. Afanyaye mema, mwanamume au mwanamke, hali yu mwaminio, basi Tutamhuisha maisha mema; na kwa yakini Tutawapa ujira wao sawa na (matendo) bora waliyokuwa wakiyatenda.

فَاِذَا قَرَاْتَ الْقُرْاٰنَ فَاسْتَعِذْ بِاللّٰهِ مِنَ الشَّيْطٰنِ الرَّجِيْمِ ﴿٩٩﴾

99. Na usomapo Qur'an, basi ujikinge kwa Allah (Akulinde) na Shetani afukuzwaye.

Aya 99. Hapa Waislamu wanaambiwa wanaposoma Qur'an wasome, *A'udhu billaahi minashshaitaanir-rajiim*, yaani "Najikinga kwa Allah anilinde na Shetani afukuzwaye."

اِنَّهٗ لَيْسَ لَهٗ سُلْطٰنٌ عَلَى الَّذِيْنَ اٰمَنُوْا وَعَلٰى رَبِّهِمْ يَتَوَكَّلُوْنَ ﴿١٠٠﴾

100. Hakika yeye hana nguvu juu ya wale walioamini na wanaomtegemea Mola wao.

اِنَّمَا سُلْطٰنُهٗ عَلَى الَّذِيْنَ يَتَوَلَّوْنَهٗ وَالَّذِيْنَ هُمْ بِهٖ مُشْرِكُوْنَ ﴿١٠٠﴾ ع ١٣ ١٩

101. Nguvu yake ni juu ya wale tu wanaomfanya rafiki na wale wanaomshirikisha (Allah).

FUNGU 14

وَاِذَا بَدَّلْنَآ اٰيَةً مَّكَانَ اٰيَةٍ ۙ وَّاللّٰهُ اَعْلَمُ بِمَا يُنَزِّلُ قَالُوْٓا اِنَّمَآ اَنْتَ مُفْتَرٍ ؕ بَلْ اَكْثَرُهُمْ لَا يَعْلَمُوْنَ ﴿١٠١﴾

102. Na Tunapoibadili Ishara mahali pa Ishara (nyingine), hali Allah ndiye Ajuaye sana Anayoyateremsha, wanasema: Wewe ni mzushi tu. Bali wengi wao hawajui.

قُلْ نَزَّلَهٗ رُوْحُ الْقُدُسِ مِنْ رَّبِّكَ بِالْحَقِّ لِيُثَبِّتَ الَّذِيْنَ اٰمَنُوْا وَهُدًى وَّبُشْرٰى لِلْمُسْلِمِيْنَ ﴿١٠٢﴾

103. Sema: Roho Takatifu ameiteremsha kutoka kwa Mola wako kwa haki, ili kuwaimarisha wale walioamini, na kuwa mwongozo na habari njema kwa waliosilimu.

وَلَقَدْ نَعْلَمُ اَنَّهُمْ يَقُوْلُوْنَ اِنَّمَا يُعَلِّمُهٗ بَشَرٌ ؕ لِسَانُ الَّذِيْ يُلْحِدُوْنَ اِلَيْهِ اَعْجَمِيٌّ وَّهٰذَا لِسَانٌ عَرَبِيٌّ مُّبِيْنٌ ﴿١٠٣﴾

104. Na bila shaka Tunajua kwamba wanasema: Yuko tu mtu anayemfundisha. Lugha ya yule wanayemwelekea ni ya kigeni na hii ni lugha ya Kiarabu iliyo bayana.

Aya hii inawaambia waaminio ya kwamba njia iliyo bora ya kuzilinda neema walizopewa na Allah ni ya kwamba waombe Mungu awalinde na mashambulio ya Shetani.

Aya 102. *Tunapoibadili Ishara,* yaani tunapoondoa Ishara (ya adhabu) au kuikawiza kwa sababu ya watu kuonyesha mabadiliko mema. Neno "Aya" lililotumiwa hapa na ambalo tumelifasiri "Ishara" kama desturi, limewafanya watu wengine wadhanie kuwa zinazobadilishwa ni Aya za Qur'an: kisha wanasema kwamba kuna Aya zilizotanguka. Katika Aya hii hakuna habari za kutanguka au kutangua Aya. Hakuna hadithi hata moja inayoeleza kuwa Mtume *s.a.w.* alipata kutaja Aya yo yote iliyotanguka, wala hakuna katika Qur'an Aya zinazopinzana zinazoweza kusemwa kuwa zimetanguana.

Aya 104. *Yuko tu mtu anayemfundisha.* Makafiri wanaposhindwa katika mabishano, hoja yao ya mwisho huwa: Muhammad alifundishwa na mtu mwingine. Hoja hii inaletwa na maadui wote wa Uislamu. Hasa mapadre wamejitahidi sana kuonyesha ya kwamba Mtume aliambiwa na watu wengine, naye akatunga Qur'an. Ukisoma vitabu vyao utashangaa jinsi walivyotanga-tanga na maneno haya ya upotevu. Dr. Rousche, katika Kitabu chake kiitwacho "Jinsi dini ya Islam ilivyotungwa," amekusanya majina ya mataifa yote aliyoyajua na ameandika ya kwamba

105. Hakika wale wasioziamini Ishara za Allah, Allah Hawaongozi, nao watapata adhabu iumizayo.

إِنَّ الَّذِينَ لَا يُؤْمِنُونَ بِآيَاتِ اللَّهِ ۙ لَا يَهْدِيهِمُ اللَّهُ وَلَهُمْ عَذَابٌ أَلِيمٌ ﴿١٠٥﴾

106. Wanaozua uwongo ni wale tu wasioziamini Ishara za Allah, na hao ndio waongo.

إِنَّمَا يَفْتَرِي الْكَذِبَ الَّذِينَ لَا يُؤْمِنُونَ بِآيَاتِ اللَّهِ ۚ وَأُولَٰئِكَ هُمُ الْكَاذِبُونَ ﴿١٠٦﴾

Mtume aliiga mafundisho ya Waarabu, Wahindi, Waparsi, Wakristo na Mayahudi. Padre Rodwell ametaja vitabu kama Mischna, Targum, Talmud, Mid. Rab, Midr Jalkut na vinginevyo na amedai kwamba mafundisho ya Qur'an yamechukuliwa toka vitabu hivyo. Huo ndio mwendo wa wakadhibishaji wote wa Mitume. Wako watu wengi ambao baada ya upelelezi mwingi wamethibitisha kwamba mafundisho ya Injili yamechukuliwa katika Torati, Talmud, na maandiko ya Wabudha.

Qur'an si Sheria ya kwanza, kwa hiyo haina budi mafundisho yake mengine yafanane na baadhi ya mafundisho yaliyomo katika Vitabu vya zamani. Injili inafanana na Taurati katika mambo mengi, kama si yote. Basi je, tuseme Yesu aliiba maneno ya Taurati akayaita Injili yake? Na kama mtu asema Musa hakufunuliwa cho chote na Mungu, bali alikwenda kaa mlimani peke yake akaandika amri kumi mwenyewe na kuwaletea wana wa Israeli, Wakristo watajibuje? Ama watu walio kabla ya Musa hawakumjua Mungu Mmoja? Au je Sheria yenye kukataza uwongo, uuaji, unyang'anyi n.k.w. mtu hawezi kuitunga pasipo kuambiwa na Mungu. Hata Waafrika, kabla ya kufikiwa na taifa lo lote walimjua Mungu, walihimiza mema na walikataza mabaya.

Hapana shaka watu walijua mambo mengi mema na mabaya kabla ya kuteremka Qur'an, lakini hawakuwa na Sheria ambayo imekusanya maneno yote na isiyo na ila yo yote. Qur'an ndicho Kitabu cha kwanza chenye sifa hii. Watu wote waliodhani kwamba Qur'an inaweza kutungwa na binadamu waliambiwa wazi wazi wakusanyike pamoja na walete sura moja tu kama ya Qur'an (sura 2:24; 11:14; 17:89; 52:35). Waarabu waliosifika Arabuni kote kwa ufasaha wao wakawa mabubu mbele ya tangazo la Qur'an. Wakristo ambao walikuwa na ujuzi mwingi wa Kiarabu hata wengine wao waliweza kutunga makamusi ya lugha hiyo, walionekana kama hawajui cho chote mbele ya Kitabu ambacho walikiita utungaji wa Muhammad. Siku hizi elimu imeongezeka sana na mapadre wamekwisha jua vitabu vyote wanavyomshuku Mtume kuvisoma, na wamekwisha tembelea nchi zote alikosafiri yeye toka utoto wake mpaka kutawafu kwake, na pia wameelewa makosa yote wanayojisingizia kuyakuta katika Qur'an, basi wakutane wote pamoja na wajaribu kuandika kitabu kama Qur'an. Lakini wasipoweza, wala hawataweza kamwe, basi waogope Moto ulioandaliwa makafiri.

Watu wanaosema ya kwamba Mtume s.a.w. aliambiwa na watu wa Kitabu, hawaelezi wale watu walikuwa na dini gani. Kama wao walimwambia Mtume hali wangali Mayahudi na Wakristo, walivumiliaje dini yao iharibiwe nao wakae kimya? Kama walisilimu, walipataje kuamini hali walijua ya kwamba yote wanayosomewa ni yale tu wanayomwandikisha Mtume? Na ikiwa walikuwa wanafiki, waliwezaje kusubiri waliposikia Qur'an ikisema kuwa wanafiki ndio wako katika daraja ya chini kabisa ya moto? Tena yeye aliwapa nini, au aliwatisha namna gani hata wakakubali kumwambia habari zote za dini zao na wasifichue siri? Linalostaajabisha zaidi ni hili ya kwamba mapadre wanasema, wasaidizi wa Mtume walikuwa wapuuzi, nao walimwambia maneno yasiyo sahihi. Mtu aliyekuwa na habari zote za Bara Arabu na Uajemi na Bara Hindi pamoja na habari zao na kajua dini zao, alishindwaje kuajiri watu wenye elimu, ambao wangeweza kumletea maandiko ya asili ya Kiyahudi na Kikristo? Hakika mashtaka haya ya mapadre ni kutaabika bure nayo ni maneno yasiyo na kichwa wala miguu.

مَنْ كَفَرَ بِاللّٰهِ مِنْۢ بَعْدِ اِيْمَانِهٖۤ اِلَّا مَنْ اُكْرِهَ وَقَلْبُهٗ مُطْمَئِنٌّۢ بِالْاِيْمَانِ وَلٰكِنْ مَّنْ شَرَحَ بِالْكُفْرِ صَدْرًا فَعَلَيْهِمْ غَضَبٌ مِّنَ اللّٰهِ ۚ وَلَهُمْ عَذَابٌ عَظِيْمٌ ﴿١٠٧﴾

107. Anayemkataa Allah baada ya kwisha kumwamini isipokuwa kwa yule ambaye ameshurutishwa hali moyo wake unatulia katika imani (hana lawama). Lakini wale ambao mioyo yao imeridhika na ukafiri, ghadhabu ya Allah itakuwa juu yao, na watapata adhabu kubwa.

ذٰلِكَ بِاَنَّهُمُ اسْتَحَبُّوا الْحَيٰوةَ الدُّنْيَا عَلَى الْاٰخِرَةِ ۙ وَاَنَّ اللّٰهَ لَا يَهْدِى الْقَوْمَ الْكٰفِرِيْنَ ﴿١٠٨﴾

108. Hayo ni kwa sababu wameyapenda zaidi maisha ya dunia kuliko Akhera, na ya kwamba Allah Hawaongozi watu makafiri.

اُولٰٓئِكَ الَّذِيْنَ طَبَعَ اللّٰهُ عَلٰى قُلُوْبِهِمْ وَسَمْعِهِمْ وَاَبْصَارِهِمْ ۚ وَاُولٰٓئِكَ هُمُ الْغٰفِلُوْنَ ﴿١٠٩﴾

109. Hao ndio Allah Amepiga muhuri juu ya mioyo yao na masikio yao na macho yao, na hao ndio waghafilikao.

لَا جَرَمَ اَنَّهُمْ فِى الْاٰخِرَةِ هُمُ الْخٰسِرُوْنَ ﴿١١٠﴾

110. Hakuna shaka ya kwamba hao ndio wenye hasara katika Akhera.

ثُمَّ اِنَّ رَبَّكَ لِلَّذِيْنَ هَاجَرُوْا مِنْۢ بَعْدِ مَا فُتِنُوْا ثُمَّ جٰهَدُوْا وَصَبَرُوْٓا ۙ اِنَّ رَبَّكَ مِنْۢ بَعْدِهَا لَغَفُوْرٌ رَّحِيْمٌ ﴿١١١﴾ ع

111. Kisha hakika Mola wako, kwa wale waliohama baada ya kuteswa, kisha wakafanya jihadi na wakasubiri, bila shaka Mola wako baada ya hayo ni Msamehevu sana, Mrehemevu.

FUNGU 15

يَوْمَ تَاْتِىْ كُلُّ نَفْسٍ تُجَادِلُ عَنْ نَّفْسِهَا وَتُوَفّٰى كُلُّ نَفْسٍ مَّا عَمِلَتْ وَهُمْ لَا يُظْلَمُوْنَ ﴿١١٢﴾

112. Siku ambayo kila nafsi itakuja kujitetea, na kila nafsi itapewa sawa na iliyoyafanya, nao hawatadhulumiwa.

وَضَرَبَ اللّٰهُ مَثَلًا قَرْيَةً كَانَتْ اٰمِنَةً مُّطْمَئِنَّةً يَّاْتِيْهَا رِزْقُهَا رَغَدًا مِّنْ كُلِّ مَكَانٍ فَكَفَرَتْ بِاَنْعُمِ اللّٰهِ فَاَذَاقَهَا اللّٰهُ لِبَاسَ الْجُوْعِ وَالْخَوْفِ بِمَا كَانُوْا يَصْنَعُوْنَ ﴿١١٣﴾

113. Na Allah Ameeleza methali ya mji uliokuwa na amani na utulivu, riziki yake ikaufikia kwa wingi kutoka kila mahali; lakini ukazikufuru neema za Allah, kwa hiyo Allah Akauonjesha vazi la njaa na hofu kwa sababu ya yale waliyokuwa wakifanya.

وَلَقَدْ جَآءَهُمْ رَسُوْلٌ مِّنْهُمْ فَكَذَّبُوْهُ فَاَخَذَهُمُ الْعَذَابُ وَهُمْ ظٰلِمُوْنَ ﴿١١٤﴾

114. Na bila shaka aliwafikia Mtume kutoka miongoni mwao; lakini wakamkadhibisha, ndipo adhabu ikawshika hali wamekuwa wadhalimu.

فَكُلُوْا مِمَّا رَزَقَكُمُ اللّٰهُ حَلٰلًا طَيِّبًا وَّاشْكُرُوْا نِعْمَتَ اللّٰهِ اِنْ كُنْتُمْ اِيَّاهُ تَعْبُدُوْنَ ﴿١١٥﴾

115. Basi kuleni katika vile Alivyowapeni Allah, vilivyo halali na twayibu (vijengavyo afya); na shukuruni neema za Allah ikiwa ninyi mnamwabudu Yeye tu.

اِنَّمَا حَرَّمَ عَلَيْكُمُ الْمَيْتَةَ وَالدَّمَ وَلَحْمَ الْخِنْزِيْرِ وَمَآ اُهِلَّ لِغَيْرِ اللّٰهِ بِهٖ ۚ فَمَنِ اضْطُرَّ غَيْرَ بَاغٍ وَّلَا عَادٍ فَاِنَّ اللّٰهَ غَفُوْرٌ رَّحِيْمٌ ﴿١١٦﴾

116. Amewaharimishieni tu nyamafu na damu na nyama ya nguruwe na achinjwaye kwa jina lisilokuwa la Allah. Lakini anayeshurutishwa, bila kuasi wala kuruka mipaka, basi hakika Allah ni Msamehevu, Mrehemevu.

وَلَا تَقُوْلُوْا لِمَا تَصِفُ اَلْسِنَتُكُمُ الْكَذِبَ هٰذَا حَلٰلٌ وَّهٰذَا حَرَامٌ لِّتَفْتَرُوْا عَلَى اللّٰهِ الْكَذِبَ ۭ اِنَّ الَّذِيْنَ يَفْتَرُوْنَ عَلَى اللّٰهِ الْكَذِبَ لَا يُفْلِحُوْنَ ﴿١١٧﴾ۭ

117. Na msiseme, kwa sababu ya uongo usemao ndimi zenu, hii ni halali na hii ni haramu, msije mkamzulia uwongo Allah. Hakika wale wamzuliao uwongo Allah hawatafaulu.

مَتَاعٌ قَلِيْلٌ ۠ وَّلَهُمْ عَذَابٌ اَلِيْمٌ ﴿١١٨﴾

118. Ni starehe ndogo nao watapata adhabu iumizayo.

وَعَلَى الَّذِيْنَ هَادُوْا حَرَّمْنَا مَا قَصَصْنَا عَلَيْكَ مِنْ قَبْلُ ۚ وَمَا ظَلَمْنٰهُمْ وَلٰكِنْ كَانُوْٓا اَنْفُسَهُمْ يَظْلِمُوْنَ ﴿١١٩﴾

119. Na ambao ni Mayahudi, zamani Tuliwaharimishia Tuliyokuhadithia. Na Sisi Hatukuwadhulumu, bali walikuwa wakijidhulumu wenyewe.

ثُمَّ اِنَّ رَبَّكَ لِلَّذِيْنَ عَمِلُوا السُّوْۗءَ بِجَهَالَةٍ ثُمَّ تَابُوْا مِنْۢ بَعْدِ ذٰلِكَ وَاَصْلَحُوْٓا ۙ اِنَّ رَبَّكَ مِنْۢ بَعْدِهَا لَغَفُوْرٌ رَّحِيْمٌ ﴿١٢٠﴾ ع ١٥

120. Kisha hakika Mola wako kwa wale waliofanya ubaya kwa ujinga, kisha wakatubia baada ya hayo na wakatenda mema, bila shaka Mola wako baada ya hayo ni Msamehevu sana, Mrehemevu.

Aya 120. *Kwa wale waliofanya ubaya kwa ujinga,* mradi wake ni kwa ujinga wa kukosa kujua au kutokuwa na utambuzi wa kiroho.

Hapa neno "kwa ujinga" limetumiwa katika maana hiyo ya pili, kwani hakuna haki kumwadhibu mtu asiye na ujuzi wa amri mojapo ambayo hakuifuata.

FUNGU 16

121. Hakika Ibrahimu, (kwa dhati yake) alikuwa (ni kama) taifa (zima), akiwa mtiifu kwa Allah, aliyehalisika; wala hakuwa miongoni mwa washirikina;

إِنَّ إِبْرٰهِيمَ كَانَ أُمَّةً قَانِتًا لِّلّٰهِ حَنِيفًا ۖ وَلَمْ يَكُ مِنَ الْمُشْرِكِينَ ﴿١٢٠﴾

122. Azishukuruye daima neema Zake; Akamchagua na kumwongoza kwenye njia iliyonyooka.

شَاكِرًا لِّأَنْعُمِهِ ۖ اجْتَبٰهُ وَهَدٰهُ إِلٰى صِرَاطٍ مُّسْتَقِيمٍ ﴿١٢١﴾

123. Na Tukampa wema katika dunia, na hakika yeye katika Akhera atakuwa miongoni mwa watu wema.

وَآتَيْنٰهُ فِي الدُّنْيَا حَسَنَةً ۖ وَإِنَّهُ فِي الْآخِرَةِ لَمِنَ الصّٰلِحِينَ ﴿١٢٢﴾

124. Kisha Tukakufunulia ya kwamba ufuate mila ya Ibrahimu (aliyekuwa) mtii kamili, wala hakuwa miongoni mwa washirikina.

ثُمَّ أَوْحَيْنَا إِلَيْكَ أَنِ اتَّبِعْ مِلَّةَ إِبْرٰهِيمَ حَنِيفًا ۖ وَمَا كَانَ مِنَ الْمُشْرِكِينَ ﴿١٢٣﴾

125. Sabato iliwekwa kama jaribio juu ya wale waliohitilafiana kwayo, na kwa hakika Mola Wako Atahukumu baina yao siku ya Kiyama kuhusu yale waliyokuwa wakihitilafiana.

إِنَّمَا جُعِلَ السَّبْتُ عَلَى الَّذِينَ اخْتَلَفُوا فِيهِ ۖ وَإِنَّ رَبَّكَ لَيَحْكُمُ بَيْنَهُمْ يَوْمَ الْقِيٰمَةِ فِيمَا كَانُوا فِيهِ يَخْتَلِفُونَ ﴿١٢٤﴾

126. Uite (watu) kwenye njia ya Mola wako kwa hekima na mawaidha mema, na ujadiliane nao kwa namna iliyo bora. Hakika Mola wako ndiye Humjua sana aliyepotea katika njia Yake, naye ndiye Awajuaye sana walioongoka.

ادْعُ إِلٰى سَبِيلِ رَبِّكَ بِالْحِكْمَةِ وَالْمَوْعِظَةِ الْحَسَنَةِ وَجَادِلْهُمْ بِالَّتِي هِيَ أَحْسَنُ ۖ إِنَّ رَبَّكَ هُوَ أَعْلَمُ بِمَنْ ضَلَّ عَنْ سَبِيلِهِ وَهُوَ أَعْلَمُ بِالْمُهْتَدِينَ ﴿١٢٥﴾

Aya 121. Ibrahimu alikuwa taifa katika nafsi yake ina maana kwamba yeye alikuwa na mbegu na uwezo uliohifadhiwa wa kuunda taifa kubwa aliloahidiwa.

Aya 125. Maudhui yako wazi. Hakuna kingine kinachojadiliwa isipokuwa Ibrahimu na ibada yake isiyotikisika na kujitolea kwake muhanga kwa ajili ya Umoja wa Allah.

Aya 126. *Bil-hikmat,* "Kwa hekima." Maana zingine za neno hili ni hizi: (1) Elimu au maarifa; (2) adili au haki; (3) uvumilivu au upole; (4) imara; (5) maneno yo yote au mafunzo yaliyo kweli sawa na hali ya wakati; (6) kipawa cha ufunuo; na (7) kinachozuia isiweko tabia ya kijinga (Akrab na Lane)

وَاِنۡ عَاقَبۡتُمۡ فَعَاقِبُوۡا بِمِثۡلِ مَا عُوۡقِبۡتُمۡ بِهٖ ؕ وَ لَئِنۡ صَبَرۡتُمۡ لَهُوَ خَيۡرٌ لِّلصّٰبِرِيۡنَ ﴿۱۲۷﴾

127. Na mkijilipiza, basi jilipizeni sawa na vile mlivyoonewa; na kama mkisubiri, hakika huo ni ubora kwa wanaosubiri.

وَاصۡبِرۡ وَ مَا صَبۡرُكَ اِلَّا بِاللّٰهِ وَلَا تَحۡزَنۡ عَلَيۡهِمۡ وَلَا تَكُ فِىۡ ضَيۡقٍ مِّمَّا يَمۡكُرُوۡنَ ﴿۱۲۸﴾

128. Na subiri, na kusubiri kwako hakuwi ila kwa (msaada wa) Allah tu; wala usiwahuzunikie, wala usiwe katika dhiki kwa sababu ya hila wanazozifanya.

اِنَّ اللّٰهَ مَعَ الَّذِيۡنَ اتَّقَوۡا وَّالَّذِيۡنَ هُمۡ مُّحۡسِنُوۡنَ ﴿۱۲۹﴾ ع

129. Kwa hakika Allah Yu pamoja na wale wanaomcha, na wale wafanyao wema.

Aya 129. Aya hii ya mwisho inaonyesha bishara ya kuwa Waislamu mwishoni watashinda, na maadui zao watashindwa, na jambo hili litaonyesha ni wao waliokuwa wacha Mungu na watendao mema, na kwamba ndio walioifuata haki.

Muttaqii (amchaye Mungu) ni mtu anayefungamana kabisa na Allah hata Mungu Mwenyewe anakuwa Mlinzi wake anayemkinga na kila maovu. *Muhsin* (mtenda wema) ni mtu ambaye baada ya yeye mwenyewe kufika chini ya ulinzi wa Allah anajaribu kuwakusanya wengine na kuwaleta chini ya ulinzi wa Allah pia. Hivyo cheo cha *muhsin* ni kikubwa zaidi kuliko cha *muttaqii.*

سُوْرَةُ بَنِيْٓ اِسْرَآءِيْلَ مَكِّيَّةٌ وَّ هِيَ مَعَ الْبَسْمَلَةِ مِائَةٌ وَّ اثْنَتَا عَشْرَةَ اٰيَةً وَّ اثْنَاعَشَرَ رُكُوْعًا

17. SURA BANII ISRAAIIL

Imeteremshwa Makka

Ina mafungu 12 na Aya 112 pamoja na Bismillahi

JUZU 15

بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ ①

1. Kwa jina la Allah, Mwingi wa rehema, Mwingi wa ukarimu.

سُبْحٰنَ الَّذِيْٓ اَسْرٰى بِعَبْدِهٖ لَيْلًا

2. Utukufu ni wa Yule Ambaye Al-impeleka mtumishi wake usiku kutoka msikiti Mtakatifu mpaka Msikiti wa Aqsa ambao Tumevibariki vilivyoko pembezoni mwake, ili Tumwonyeshe baadhi ya Ishara Zetu. Hakika Yeye Ndiye Mwenye kusikia, Mwenye kuona.

مِّنَ الْمَسْجِدِ الْحَرَامِ اِلَى الْمَسْجِدِ الْاَقْصَا
الَّذِيْ بٰرَكْنَا حَوْلَهٗ لِنُرِيَهٗ مِنْ اٰيٰتِنَا ؕ
اِنَّهٗ هُوَ السَّمِيْعُ الْبَصِيْرُ ②

وَاٰتَيْنَا مُوْسَى الْكِتٰبَ وَجَعَلْنٰهُ هُدًى

3. Na Tulimpa Musa Kitabu, na Tukakifanya mwongozo kwa wana wa Israeli, (wakiambiwa): Msishike mlinzi badala Yangu.

لِّبَنِيْٓ اِسْرَآءِيْلَ اَلَّا تَتَّخِذُوْا مِنْ دُوْنِيْ
وَكِيْلًا ③

Sura hii imeitwa *Banii Israaiil* kwa sababu inaeleza mambo ya maana katika historia ya wana wa Israeli na mambo yaliyowapitia katika dini. Pia inaitwa *Israa* kwa kuwa imeanza na habari ya Njozi kuu ya Mtume *s.a.w.* inayohusu Safari ya Usiku aliyokwenda Yerusalem ambayo ni mojawapo katika mambo makubwa yaliyoelezwa katika sura hii.

Baadhi ya wafasiri wanaeleza ya kuwa rai ya wanazuoni wa Kiislamu inakubali ya kuwa sura hii yote ni ya Makka (Muhit), lakini wanazuoni wengine wanaona ya kuwa Aya 2-8 ni za Madina.

Aya 2. Aya hii inaeleza habari ya *Israa* (safari ya usiku) ya Mtume *s.a.w.* Katika Aya 61 safari hii ya usiku imeitwa *Ru'yaa* (yaani, Njozi); hivyo tunakuta ya kuwa masahaba kadha wa kadha na baadhi ya wanachuoni wa baadaye wa Kiislamu, kwa mujibu wa Aya hii ya 61 wamesema kuwa *Israa* ni njozi. Kwa mfano Ibni Is'hak na Ibni Jarir wanaeleza ya kwamba Mu'aawiya alipoulizwa habari za *Israa* alijibu ya kwamba ilikuwa ni njozi ambayo ilikuja tokea kuwa kweli (Manthur, jalada 4 uk. 197). Bi Aisha pia, inaelezwa, alikuwa na maoni hayo hayo (Hisham na Ma'aad, jalada 1).

Njozi hii ilikuwa bishara. Kusafiri kwenda *msikiti ulio mbali* mradi wake ni kuhamia kwa Mtume Madina ambako ilikuwa ajenge msikiti ambao ulikadiriwa baadaye uwe Kituo cha Dini zote. Na Mtume *s.a.w.* kujiona katika njozi anawasalisha Manabii wote waliokufa zamani mradi wake ni kuwa hii Dini mpya ya Islam ilikuwa ya kuenea dunia nzima na wafuasi wa kila dini kuiingia. Kadhalika kwenda Yerusalem katika njozi mradi wake unaweza kuwa ya kwamba atatawala katika nchi ile. Bishara hii ilitimia katika siku za Ukhalifa wa Seyidna Umar.

ذُرِّيَّةَ مَنْ حَمَلْنَا مَعَ نُوْحٍ ؕ اِنَّهٗ كَانَ عَبْدًا شَكُوْرًا ۝٤

4. (Na pia Tuliwaambia) wazao wa wale Tuliowapandisha (katika jahazi) pamoja na Nuhu. Hakika yeye alikuwa Mtumishi mwenye shukurani nyingi.

وَقَضَيْنَآ اِلٰى بَنِيْٓ اِسْرَآءِيْلَ فِى الْكِتٰبِ لَتُفْسِدُنَّ فِى الْاَرْضِ مَرَّتَيْنِ وَلَتَعْلُنَّ عُلُوًّا كَبِيْرًا ۝٥

5. Na Tukawafunulia wana wa Israeli katika Kitabu: Bila shaka ninyi mtafanya uharibifu katika ardhi mara mbili, na kwa yakini mtaasi uasi mkubwa.

فَاِذَا جَآءَ وَعْدُ اُوْلٰىهُمَا بَعَثْنَا عَلَيْكُمْ عِبَادًا لَّنَآ اُولِىْ بَاْسٍ شَدِيْدٍ فَجَاسُوْا خِلٰلَ الدِّيَارِ ؕ وَكَانَ وَعْدًا مَّفْعُوْلًا ۝٦

6. Basi ilipofika ahadi ya kwanza ya hizo mbili, Tukawapelekea watumishi Wetu waliokuwa na nguvu kubwa za kivita ambao walipenya ndani kabisa katika vijiji wakifanya maangamizi, na hii ilikuwa ahadi itimizwayo.

ثُمَّ رَدَدْنَا لَكُمُ الْكَرَّةَ عَلَيْهِمْ وَاَمْدَدْنٰكُمْ بِاَمْوَالٍ وَّبَنِيْنَ وَجَعَلْنٰكُمْ اَكْثَرَ نَفِيْرًا ۝٧

7. Kisha Tukawarudishieni nguvu juu yao, na Tukawasaidieni kwa mali na watoto, na Tukawafanyeni kundi kubwa sana.

اِنْ اَحْسَنْتُمْ اَحْسَنْتُمْ لِاَنْفُسِكُمْ ۖ وَاِنْ اَسَاْتُمْ فَلَهَا ؕ فَاِذَا جَآءَ وَعْدُ الْاٰخِرَةِ لِيَسُوْٓءٗا وُجُوْهَكُمْ وَلِيَدْخُلُوا الْمَسْجِدَ كَمَا دَخَلُوْهُ اَوَّلَ مَرَّةٍ وَّلِيُتَبِّرُوْا مَا عَلَوْا تَتْبِيْرًا ۝٨

8. Kama mkifanya wema, mtajifanyia wema nafsi zenu; na kama mkifanya ubaya, basi mtajifanyia wenyewe. Na ilipofika ahadi ya mwisho (Tukawapelekeeni watu) ili wawafanye vibaya wakubwa wenu na wauingie msikiti kama walivyouingia mara ya kwanza na wayaangamize kabisa waliyoyashinda·

Aya 6. *Ilipofika ahadi ya kwanza.* Msiba wa kwanza uliwafikia Waisraeli baada ya Nabii Daudi na wa pili baada ya Nabii Isa.

Aya 8. Aya hii inaeleza habari za Mayahudi kuangukia katika maovu mara ya pili na adhabu zilizowafikia kwa makosa hayo. Walimsulubisha Nabii Isa wakitaka kumwua kifo cha laana cha msalabani, na wakauvunja Mwendeleo wake. Hivyo Allah akawafikishia adhabu ya kutisha wakati majeshi ya Warumi yaliyoongozwa na Titus katika mwaka 70 A.D yalipoharibu nchi na kwa kitisho kisicho na mfano mji wa Yerusalem ukateketezwa, na Hekalu la Nabii Suleimani likachomwa na kuanguka (Enc. Bib., chini ya Yerusalem).

عَسٰى رَبُّكُمْ اَنْ يَّرْحَمَكُمْ ۚ وَاِنْ عُدْتُّمْ
عُدْنَا ۘ وَجَعَلْنَا جَهَنَّمَ لِلْكٰفِرِيْنَ حَصِيْرًا ۝٨

9. (Hata sasa) huenda Mola wenu Akawarehemuni; na kama mtarudia (mwendo wenu wa kwanza), Sisi pia Tutarudia; na Tumeifanya Jahanamu kuwa gereza kwa ajili ya makafiri.

اِنَّ هٰذَا الْقُرْاٰنَ يَهْدِيْ لِلَّتِيْ هِيَ اَقْوَمُ
وَيُبَشِّرُ الْمُؤْمِنِيْنَ الَّذِيْنَ يَعْمَلُوْنَ
الصّٰلِحٰتِ اَنَّ لَهُمْ اَجْرًا كَبِيْرًا ۝٩

10. Hakika Qur'an hii inaongoza kwenye yale yaliyonyooka kabisa; na inawapa habari njema waaminio, wafanyao vitendo vizuri, ya kwamba watapata malipo makubwa.

وَّاَنَّ الَّذِيْنَ لَا يُؤْمِنُوْنَ بِالْاٰخِرَةِ اَعْتَدْنَا
لَهُمْ عَذَابًا اَلِيْمًا ۝١٠

11. Na ya kwamba wale wasioiamini Akhera Tumewaandalia adhabu iumizayo.

FUNGU 2

وَيَدْعُ الْاِنْسَانُ بِالشَّرِّ دُعَآءَهٗ بِالْخَيْرِ ؕ
وَكَانَ الْاِنْسَانُ عَجُوْلًا ۝١١

12. Na mwanadamu huomba shari kama vile aombavyo heri; na mwanadamu ni mwenye haraka sana.

وَجَعَلْنَا الَّيْلَ وَالنَّهَارَ اٰيَتَيْنِ فَمَحَوْنَآ
اٰيَةَ الَّيْلِ وَجَعَلْنَآ اٰيَةَ النَّهَارِ مُبْصِرَةً
لِّتَبْتَغُوْا فَضْلًا مِّنْ رَّبِّكُمْ وَلِتَعْلَمُوْا
عَدَدَ السِّنِيْنَ وَالْحِسَابَ ؕ وَكُلَّ شَيْءٍ
فَصَّلْنٰهُ تَفْصِيْلًا ۝١٢

13. Na Tumefanya usiku na mchana kuwa Ishara mbili; kisha Tumeifuta Ishara ya usiku na Tukaifanya Ishara ya mchana iangazayo, ili mtafute fadhili itokayo kwa Mola wenu, na mpate kujua idadi ya miaka na hesabu; na kila kitu Tumekieleza waziwazi.

وَكُلَّ اِنْسَانٍ اَلْزَمْنٰهُ طٰٓئِرَهٗ فِيْ عُنُقِهٖ ؕ
وَنُخْرِجُ لَهٗ يَوْمَ الْقِيٰمَةِ كِتٰبًا يَّلْقٰىهُ
مَنْشُوْرًا ۝١٣

14. Na kila mwanadamu Tumemfungia matendo yake shingoni mwake; na Tutamtolea siku ya Kiyama daftari atakayoikuta imekunjuliwa.

Aya 12. *Na mwanadamu huomba shari kama vile aombavyo heri.* Siyo mradi wa Aya hii kuwa kuna mtu ambaye anaweza kuwa mpumbavu hata afike kumwomba Mungu ampelekee ubaya. Mradi wake ni huu kwamba mwanadamu humwomba Allah kwa maneno ya mdomo kuwa ampe heri, hali kwa matendo yake mabaya anaikaribisha chuki na adhabu ya Mungu. Na namna hii matendo yake yanakadhibisha maneno yake.

Aya 14. *Na kila mwanadamu Tumemfungia matendo yake shingoni mwake.* Ndiyo kusema, hakuna tendo lo lote la mtu linalopotea bure; kila tendo lake lazima litoe matunda, mema au mabaya. Kufunga matendo yake shingoni mwake inaonyesha kwamba matendo yake yatamng'ang'ania moja kwa moja, na matokeo yake yatakuwa pamoja naye daima.

15. Soma daftari yako. Nafsi yako inakutosha leo kukuhesabia.

اِقْرَاْ كِتٰبَكَ ؕ كَفٰى بِنَفْسِكَ الْيَوْمَ عَلَيْكَ حَسِيْبًا ﴿١٥﴾

16. Anayeongoka, basi anaongoka kwa ajili ya nafsi yake tu; na anayepotea, basi anapotea kwa hasara (ya nafsi) yake. Wala hatabeba mbebaji mzigo wa mwingine. Nasi si waadhibishao mpaka Tumepeleka Mtume.

مَنِ اهْتَدٰى فَاِنَّمَا يَهْتَدِيْ لِنَفْسِهٖ ۚ وَمَنْ ضَلَّ فَاِنَّمَا يَضِلُّ عَلَيْهَا ؕ وَلَا تَزِرُ وَازِرَةٌ وِّزْرَ اُخْرٰى ؕ وَمَا كُنَّا مُعَذِّبِيْنَ حَتّٰى نَبْعَثَ رَسُوْلًا ﴿١٦﴾

17. Na Tunapokusudia kuuangamiza mji tunawaachia wenye uwezo wa kiuchumi miongoni mwao (kufanya watakavyo). Kisha wanajiingiza katika mambo yote ya dhambi yaliyo humo, hapo kauli inahakiki juu yake ndipo Tunauangamiza maangamizo makubwa.

وَاِذَاۤ اَرَدْنَاۤ اَنْ نُّهْلِكَ قَرْيَةً اَمَرْنَا مُتْرَفِيْهَا فَفَسَقُوْا فِيْهَا فَحَقَّ عَلَيْهَا الْقَوْلُ فَدَمَّرْنٰهَا تَدْمِيْرًا ﴿١٧﴾

18. Na vingapi Tumeviangamiza katika vizazi baada ya Nuhu! Na Mola wako Anatosha kwa dhambi za watu Wake kuwa Mwenye habari, Aonaye.

وَكَمْ اَهْلَكْنَا مِنَ الْقُرُوْنِ مِنْۢ بَعْدِ نُوْحٍ ؕ وَكَفٰى بِرَبِّكَ بِذُنُوْبِ عِبَادِهٖ خَبِيْرًا ۢ بَصِيْرًا ﴿١٨﴾

19. Anayetaka (dunia hii) ipitayo upesi, Tutamharakishia humo Tunayoyataka - kwa yule Tumtakaye; kisha Tumemfanyia Jahanamu, ataiingia akidharauliwa, akifukuzwa.

مَنْ كَانَ يُرِيْدُ الْعَاجِلَةَ عَجَّلْنَا لَهٗ فِيْهَا مَا نَشَآءُ لِمَنْ نُّرِيْدُ ثُمَّ جَعَلْنَا لَهٗ جَهَنَّمَ ۚ يَصْلٰىهَا مَذْمُوْمًا مَّدْحُوْرًا ﴿١٩﴾

20. Na aliyetaka Akhera na kuifanyia juhudi - juhudi inayopasa, naye yu mumini, basi hao ndio juhudi yao itakubaliwa.

وَمَنْ اَرَادَ الْاٰخِرَةَ وَسَعٰى لَهَا سَعْيَهَا وَهُوَ مُؤْمِنٌ فَاُولٰٓئِكَ كَانَ سَعْيُهُمْ مَّشْكُوْرًا ﴿٢٠﴾

21. Wote Tunawasaidia, hawa na hawa, ikiwa zawadi toka kwa Mola wako; na zawdi ya Mola Wako si yenye kuzuiliwa.

كُلًّا نُّمِدُّ هٰٓؤُلَآءِ وَهٰٓؤُلَآءِ مِنْ عَطَآءِ رَبِّكَ ؕ وَمَا كَانَ عَطَآءُ رَبِّكَ مَحْظُوْرًا ﴿٢١﴾

Aya 16. *Wala hatabeba mbebaji mzigo wa mwingine,* mradi wake ni kuwa kila mtu atapata matokeo ya matendo yake. Mtu mwingine hatahukumiwa kwa kosa lisilokuwa lake.

Nasi si waadhibishao mpaka Tumepeleka Mtume. Hii ni kanuni nyingine ya Allah ya kuwa hawaadhibu watu mpaka amewatumia Mwonyaji. Kanuni hii pia imeelezwa katika sura hizi: 67:9-10; 39:72; 35:38 na 28:60.

Aya 21. Aya hii inaondoa wasiwasi ambao ungeweza kutokea kwa kusoma Aya ya 19

22. Tazama jinsi Tulivyowafadhili baadhi yao kuliko wengine; na bila shaka Akhera ni yenye vyeo vikubwa zaidi, na yenye fadhili kubwa zaidi.

اُنْظُرْ كَيْفَ فَضَّلْنَا بَعْضَهُمْ عَلٰى بَعْضٍ ؕ وَلَلْاٰخِرَةُ اَكْبَرُ دَرَجٰتٍ وَّ اَكْبَرُ تَفْضِيْلًا ﴿٢١﴾

23. Usifanye mungu mwingine pamoja na Allah usije ukakaa hali ya kudharauliwa (na) kutupwa.

لَا تَجْعَلْ مَعَ اللّٰهِ اِلٰهًا اٰخَرَ فَتَقْعُدَ مَذْمُوْمًا مَّخْذُوْلًا ﴿٢٢﴾ ع ٢

FUNGU 3

24. Na Mola wako Ameagiza kuwa msimwabudu ye yote ila Yeye tu, na kufanya wema kwa wazazi; kama mmoja wao akifikia uzee ukiwa naye, au wote wawili, basi usiwaambie hata aakh wala usiwakemee, na useme nao kwa msemo wa heshima.

وَقَضٰى رَبُّكَ اَلَّا تَعْبُدُوْٓا اِلَّآ اِيَّاهُ وَبِالْوَالِدَيْنِ اِحْسَانًا ؕ اِمَّا يَبْلُغَنَّ عِنْدَكَ الْكِبَرَ اَحَدُهُمَآ اَوْ كِلٰهُمَا فَلَا تَقُلْ لَّهُمَآ اُفٍّ وَّ لَا تَنْهَرْهُمَا وَقُلْ لَّهُمَا قَوْلًا كَرِيْمًا ﴿٢٣﴾

---

kwamba ni matendo ya waaminio tu yanayopewa malipo. Aya hii inatuambia kwamba msaada wa Allah ni wa namna mbili: (1) Msaada wa jamii, unaofanya matendo na juhudi zilizo njema za watu wote, Waislamu, Wakristo, Mayahudi, Mabanyani n.k.w. yalete faida sawa na kadiri yalivyo, na (2) fadhili maalumu na msaada maalumu wa Allah unaohusu mambo ya kiroho na ambao hupewa watumishi wakweli tu wa Allah, na wananyimwa wasioamini.

Aya 24. Mtume *s.a.w.* kwa mujibu wa Aya za Qur'an alitia mkazo kuwatumikia wazazi kwa huruma na wema. Safari moja mtu mmoja alimwuliza: "Haki ya wazazi ni nini?" Mtume *s.a.w.* alijibu, "Wazazi - mama na baba, ndio Pepo kwa ajili yako na ndio Moto kwa ajili yako" (Kashful-Ghummah). Yaani , kama utawatumikia vizuri utapata Pepo, waila, Moto. Pia inasimuliwa ya kuwa Mtume *s.a.w.* alikuwa anasema: "Anayependa ya kuwa umri wake uzidi, na riziki yake ikunjuke, basi awafanyie wema wazazi wake, auunganishe ujamaa wake" (Kashful-Ghummah). Ibni Abbas anasema ya kuwa safari moja mtu mmoja alifika kwa Mtume *s.a.w.* na akamhadithia akasema: "Mimi nimefanya dhambi kubwa. Je naweza kutubu?" Mtume *s.a.w.* akamwuliza, Je, unaye mama? Akajibu, La. Akamwuliza, Unaye mama mkubwa au mama mdogo? Akasema, Naam. Mtume *s.a.w.* akasema, Basi umtendee wema.

Katika Hadithi nyingine imesimuliwa ya kuwa Mtume *s.a.w.* alisema, "Amefedheheka, Amefedheheka. Mtu akamwuliza, Nani? Mtume *s.a.w.* akamjibu, Yule ambaye ana baba na mama, wote wawili au mmoja wao katika uzee wao, kisha hakuwafanyia wema na kuingia Peponi" (Kashful-Ghummah).

وَاخْفِضْ لَهُمَا جَنَاحَ الذُّلِّ مِنَ الرَّحْمَةِ وَقُلْ رَّبِّ ارْحَمْهُمَا كَمَا رَبَّيٰنِيْ صَغِيْرًا ﴿٢٥﴾

25. Na uwainikie bawa la unyenyekevu kwa huruma. Na useme: Mola wangu, Uwarehemu kama walivyonilea katika utoto.

رَبُّكُمْ اَعْلَمُ بِمَا فِيْ نُفُوْسِكُمْ ؕ اِنْ تَكُوْنُوْا صٰلِحِيْنَ فَاِنَّهٗ كَانَ لِلْاَوَّابِيْنَ غَفُوْرًا ﴿٢٦﴾

26. Mola wenu Anajua sana yaliyomo mioyoni mwenu; kama mkiwa wema, basi hakika Yeye ndiye Mwenye kughofiria waelekeao.

وَاٰتِ ذَا الْقُرْبٰى حَقَّهٗ وَالْمِسْكِيْنَ وَابْنَ السَّبِيْلِ وَلَا تُبَذِّرْ تَبْذِيْرًا ﴿٢٧﴾

27. Na umpe ndugu haki yake, na maskini na msafiri, wala usitapanye (mali yako) kwa ubadhirifu.

اِنَّ الْمُبَذِّرِيْنَ كَانُوْٓا اِخْوَانَ الشَّيٰطِيْنِ ؕ وَكَانَ الشَّيْطٰنُ لِرَبِّهٖ كَفُوْرًا ﴿٢٨﴾

28. Hakika watumiao kwa ubadhirifu ni ndugu za mashetani; na Shetani ndiye asiyemshukuru Mola wake.

وَاِمَّا تُعْرِضَنَّ عَنْهُمُ ابْتِغَآءَ رَحْمَةٍ مِّنْ رَّبِّكَ تَرْجُوْهَا فَقُلْ لَّهُمْ قَوْلًا مَّيْسُوْرًا ﴿٢٩﴾

29. Na kama unatengana nao kwa kutafuta rehema ya Mola wako unayoitumai, basi sema nao kwa maneno laini.

وَلَا تَجْعَلْ يَدَكَ مَغْلُوْلَةً اِلٰى عُنُقِكَ وَلَا تَبْسُطْهَا كُلَّ الْبَسْطِ فَتَقْعُدَ مَلُوْمًا مَّحْسُوْرًا ﴿٣٠﴾

30. Na wala usiufanye mkono wako ufungiwe shingoni mwako (kwa ubakhili uliokithiri), wala usiukunjue wote (kwa ubadhirifu mkubwa); usije ukaishia katika hali ya kulaumiwa na kujuta.

Aya 25. Maneno ya dua iliyo katika Aya hii yanafahamisha ya kuwa katika uzee wazazi wanatakiwa kulelewa kwa uangalifu na upenzi kama wanavyolelewa watoto wadogo.

Aya 27. *Ndugu.* Abu Huraira anasimulia ya kuwa Mtume *s.a.w.* alikuwa anasema, "Anayemwamini Mwenyezi Mungu na siku ya Kiyama basi aunganishe ujamaa." Tena alisema, "Anayependa ya kuwa riziki yake izidishwe na heshima yake ikae siku nyingi, basi aunganishe ujamaa" (Kashful-Ghummah). Katika hadithi nyingine na katika Aya za Qur'an watu wamehimizwa kuangalia udugu na ujamaa.

Msafiri. Mtume *s.a.w.* alisema ya kuwa msafiri anayo haki akaribishwe katika chakula kwa siku tatu bure mahali atakapofika, na kama ananyimwa ana haki ya kutumia nguvu sawa na akili (Dawud, *Kitabul-At'ima).*

Fundisho hili linaweza kutendeka katika nchi ambayo Sheria ya Kiislamu imetawala, maana kwa mujibu wa fundisho hili wenyeji wa mahali wote wanalazimika kumkaribisha msafiri. Kama fundisho hili lingefuatwa, maovu mengi yanayopatikana katika mahoteli na mikahawa yangetoweka.

Aya 30. Aya hii inafundisha njia ya sawa ya mtu kutumia pesa zake. Asiwe bahili na kuacha kuzitumia hata kama anayo haja ya haki, wala asizitumie kwa kuzisambaza ovyo, bali ashike njia ya katikati.

31. Hakika Mola wako Humkunjulia riziki Amtakaye na Hudhikisha. Hakika Yeye kwa watumishi Wake ni Mwenye habari, Aonaye.

إِنَّ رَبَّكَ يَبْسُطُ الرِّزْقَ لِمَنْ يَّشَآءُ وَيَقْدِرُ ؕ اِنَّهٗ كَانَ بِعِبَادِهٖ خَبِيْرًا بَصِيْرًا ﴿٣١﴾ ع

FUNGU 4

32. Wala msiwaue watoto wenu kwa kuogopa umaskini. Sisi ndio Tunaowaruzuku wao na ninyi pia. Kwa yakini kuwaua ni hatia kubwa.

وَلَا تَقْتُلُوْٓا اَوْلَادَكُمْ خَشْيَةَ اِمْلَاقٍ ؕ نَحْنُ نَرْزُقُهُمْ وَاِيَّاكُمْ ؕ اِنَّ قَتْلَهُمْ كَانَ خِطْاً كَبِيْرًا ﴿٣٢﴾

33. Wala msikaribie zinaa. Hakika hiyo ni kinyaa na ni njia mbaya.

وَلَا تَقْرَبُوا الزِّنٰٓى اِنَّهٗ كَانَ فَاحِشَةً ؕ وَسَآءَ سَبِيْلًا ﴿٣٣﴾

34. Wala msiiue nafsi ambayo Allah Amekataza, isipokuwa kwa haki. Na mwenye kuuawa kwa kudhulumiwa, basi Tumeweka mamlaka kwa mrithi wake, hivyo asipite kiasi katika kuua; hakika yeye atasaidiwa.

وَلَا تَقْتُلُوا النَّفْسَ الَّتِىْ حَرَّمَ اللّٰهُ اِلَّا بِالْحَقِّ ؕ وَمَنْ قُتِلَ مَظْلُوْمًا فَقَدْ جَعَلْنَا لِوَلِيِّهٖ سُلْطٰنًا فَلَا يُسْرِفْ فِّى الْقَتْلِ ؕ اِنَّهٗ كَانَ مَنْصُوْرًا ﴿٣٤﴾

35. Wala msikaribie mali ya yatima, isipokuwa kwa njia iliyo bora, mpaka afikie balehe yake, na timizeni ahadi. Kwa hakika ahadi itaulizwa.

وَلَا تَقْرَبُوْا مَالَ الْيَتِيْمِ اِلَّا بِالَّتِىْ هِىَ اَحْسَنُ حَتّٰى يَبْلُغَ اَشُدَّهٗ ۪ وَاَوْفُوْا بِالْعَهْدِ ۚ اِنَّ الْعَهْدَ كَانَ مَسْئُوْلًا ﴿٣٥﴾

Aya 32. Aya hii inakataza kufanya ubahili katika kuwaelimisha na kuwakuza watoto vizuri, maana watoto wasiolishwa na kuvishwa vizuri mara nyingi hufa kwa maradhi. Kadhalika kuwanyima watoto elimu ni kama kuwaua, watakuwa wafu katika mambo ya elimu na katika tabia zao.

Aya hii haisemi habari za mila ya Waarabu ya kuua watoto wa kike ambayo imetajwa katika sura 16:59, 60 na 43:18 na kusemwa kuwa sababu iliyowafanya wawaue binti zao ni kuogopa fedheha na fahari ya uwongo. Lakini sababu iliyotolewa hapa ni kwamba msiue watoto kwa kuogopa umaskini, maana hakuna mpumbavu ambaye anaweza kumpa sumu au kumnyonga au kumchinja mtoto wake baada ya kumzaa kwa kuogopa umaskini. Jambo analoweza kufanya ni kuacha kutoa matumizi mema kwa sababu ya ubahili na kuogopa mali zisiishe akawa maskini.

Kadhalika kuua watoto kunaweza kuwa katika sura ya mtu kuzuia kizazi, ambalo ni jambo lililoruhusiwa ikiwa mwanamke anaweza kufa kwa kuzaa.

Aya 33. Qur'an haisemi kama Biblia, "Usizini;" bali inasema, "Msiikaribie zinaa," ambayo ni amri pana zaidi na inayofaa zaidi. Amri ya Islam inataka mtu asikaribie zinaa kwa kukaribia mambo yanayoweza kumshawishi afanye tendo hilo ovu, kama wanawake na wanaume kuchanganyika ovyo.

Aya 35. Aya hii inaeleza waziwazi ya kuwa mali ya yatima iangaliwe kwa namna itakayoifanya iweze kuzidi. Hapa pia mafundisho ya dini ya Kiislamu yanashinda dini zingine. Hakuna dini nyingine yo yote iliyotoa maelezo mengi namna hii kwa kulinda mali ya mayatima.

وَاَوْفُوا الْكَيْلَ اِذَا كِلْتُمْ وَزِنُوْا بِالْقِسْطَاسِ الْمُسْتَقِيْمِ ؕ ذٰلِكَ خَيْرٌ وَّاَحْسَنُ تَاْوِيْلًا ﴿۳۵﴾

36. Na timizeni kipimo mpimapo, na pimeni kwa mizani iliyo sawa. Hayo ni wema na bora mwishoni.

وَلَا تَقْفُ مَا لَيْسَ لَكَ بِهٖ عِلْمٌ ؕ اِنَّ السَّمْعَ وَالْبَصَرَ وَالْفُؤَادَ كُلُّ اُولٰٓئِكَ كَانَ عَنْهُ مَسْئُوْلًا ﴿۳۶﴾

37. Wala usifuate usiyo na elimu nayo. Hakika masikio na macho na moyo - hivyo vyote vitaulizwa.

وَلَا تَمْشِ فِى الْاَرْضِ مَرَحًا ۚ اِنَّكَ لَنْ تَخْرِقَ الْاَرْضَ وَلَنْ تَبْلُغَ الْجِبَالَ طُوْلًا ﴿۳۷﴾

38. Wala usitembee katika ardhi kwa maringo; hakika wewe huwezi kuipasua ardhi, wala huwezi kufikia urefu wa milima.

كُلُّ ذٰلِكَ كَانَ سَيِّئُهٗ عِنْدَ رَبِّكَ مَكْرُوْهًا ﴿۳۸﴾

39. Haya yote ubaya wake mbele ya Mola wako ni uchukizao.

ذٰلِكَ مِمَّاۤ اَوْحٰۤى اِلَيْكَ رَبُّكَ مِنَ الْحِكْمَةِ ؕ وَلَا تَجْعَلْ مَعَ اللّٰهِ اِلٰهًا اٰخَرَ فَتُلْقٰى فِىْ جَهَنَّمَ مَلُوْمًا مَّدْحُوْرًا ﴿۳۹﴾

40. Hayo ni katika yale Aliyokufunulia Mola wako katika hekima. Wala usiweke pamoja na Allah, mungu mwingine, usije kutupwa katika Jahanamu hali ya kulaumiwa (na) kufukuzwa.

اَفَاَصْفٰىكُمْ رَبُّكُمْ بِالْبَنِيْنَ وَاتَّخَذَ مِنَ الْمَلٰٓئِكَةِ اِنَاثًا ؕ اِنَّكُمْ لَتَقُوْلُوْنَ قَوْلًا عَظِيْمًا ﴿۴۰﴾ ع

41. Je, Mola wenu Amewachagulieni watoto wanaume na Mwenyewe Akajichukulia wasichana miongoni mwa Malaika? Kwa hakika ninyi mnasema maneno makubwa.

FUNGU 5

وَلَقَدْ صَرَّفْنَا فِىْ هٰذَا الْقُرْاٰنِ لِيَذَّكَّرُوْا ؕ وَمَا يَزِيْدُهُمْ اِلَّا نُفُوْرًا ﴿۴۱﴾

42. Na Tumekwisha eleza (kila jambo) katika Qur'an hii kwa namnanamna ili wapate kukumbuka; lakini haiwazidishii ila kuchukia.

قُلْ لَّوْ كَانَ مَعَهٗۤ اٰلِهَةٌ كَمَا يَقُوْلُوْنَ اِذًا لَّابْتَغَوْا اِلٰى ذِى الْعَرْشِ سَبِيْلًا ﴿۴۲﴾

43. Sema: Lau wangalikuwa pamoja naye waungu (wengine) kama wasemavyo, hapo wangalitafuta njia ya kufikia kwa Mwenye enzi.

سُبْحٰنَهٗ وَتَعٰلٰى عَمَّا يَقُوْلُوْنَ عُلُوًّا كَبِيْرًا ﴿۴۳﴾

44. Yeye ni Mtakatifu, na Yu juu ya hayo wasemayo, kwa utukufu mkubwa.

تُسَبِّحُ لَهُ السَّمٰوٰتُ السَّبْعُ وَالْاَرْضُ وَمَنْ فِيْهِنَّ ؕ وَاِنْ مِّنْ شَىْءٍ اِلَّا يُسَبِّحُ

45. Zinamtukuza mbingu saba na ardhi na vilivyomo ndani yao; na hakuna cho chote isipokuwa kinamsabihi kwa

بِحَمْدِهٖ وَلٰكِنْ لَّا تَفْقَهُوْنَ تَسْبِيْحَهُمْ ؕ
اِنَّهٗ كَانَ حَلِيْمًا غَفُوْرًا ﴿٤٤﴾

sifa Zake njema; lakini ninyi hamfahamu kutukuza kwao. Hakika Yeye ni Mpole, Anayesamehe.

وَاِذَا قَرَاْتَ الْقُرْاٰنَ جَعَلْنَا بَيْنَكَ وَبَيْنَ
الَّذِيْنَ لَا يُؤْمِنُوْنَ بِالْاٰخِرَةِ حِجَابًا
مَّسْتُوْرًا ۙ﴿٤٥﴾

46. Na unaposoma Qur'an, Tunatia baina yako na baina ya wale wasioamini Akhera pazia iliyostiriwa.

وَّجَعَلْنَا عَلٰى قُلُوْبِهِمْ اَكِنَّةً اَنْ
يَّفْقَهُوْهُ وَفِيْٓ اٰذَانِهِمْ وَقْرًا ؕ وَاِذَا
ذَكَرْتَ رَبَّكَ فِى الْقُرْاٰنِ وَحْدَهٗ
وَلَّوْا عَلٰٓى اَدْبَارِهِمْ نُفُوْرًا ﴿٤٦﴾

47. Na Tumetia vifuniko mioyoni mwao ili wasiifahamu na masikio yao Tukayatia uziwi. Na unapomtaja Mola wako wa Pekee katika Qur'an, basi wao hugeuza migongo yao kwa chuki.

نَحْنُ اَعْلَمُ بِمَا يَسْتَمِعُوْنَ بِهٖٓ
اِذْ يَسْتَمِعُوْنَ اِلَيْكَ وَاِذْ هُمْ نَجْوٰٓى
اِذْ يَقُوْلُ الظّٰلِمُوْنَ اِنْ تَتَّبِعُوْنَ اِلَّا
رَجُلًا مَّسْحُوْرًا ﴿٤٧﴾

48. Tunajua sana kwa nini wanasikiliza, wanapokusikiliza na wanapong'ona, wadhalimu wanaposema: Ninyi hamumfuati isipokuwa mtu aliyelogwa.

اُنْظُرْ كَيْفَ ضَرَبُوْا لَكَ الْاَمْثَالَ
فَضَلُّوْا فَلَا يَسْتَطِيْعُوْنَ سَبِيْلًا ﴿٤٨﴾

49. Tazama jinsi wanavyokupigia mifano; basi wamepotea, hivyo hawawezi kupata njia.

وَقَالُوْٓا ءَاِذَا كُنَّا عِظَامًا وَّرُفَاتًا ءَاِنَّا
لَمَبْعُوْثُوْنَ خَلْقًا جَدِيْدًا ﴿٤٩﴾

50. Na wakasema: Je, tutakapokuwa mifupa na chembe zilizosagika, je, tutafufuliwa kuwa viumbe wapya?

قُلْ كُوْنُوْا حِجَارَةً اَوْ حَدِيْدًا ﴿٥٠﴾

51. Sema: Kuweni mawe au chuma,

اَوْ خَلْقًا مِّمَّا يَكْبُرُ فِىْ صُدُوْرِكُمْ ۚ
فَسَيَقُوْلُوْنَ مَنْ يُّعِيْدُنَا ؕ قُلِ الَّذِىْ
فَطَرَكُمْ اَوَّلَ مَرَّةٍ ۚ فَسَيُنْغِضُوْنَ
اِلَيْكَ رُءُوْسَهُمْ وَيَقُوْلُوْنَ مَتٰى هُوَ ؕ
قُلْ عَسٰٓى اَنْ يَّكُوْنَ قَرِيْبًا ﴿٥١﴾

52. Au kiumbe katika vile vinavyoonekana vigumu katika mioyo yenu (hata hivyo mtafufuliwa). Hapo watasema: Ni nani atakayeturudisha? Sema: Ambaye Aliwaumbeni mara ya kwanza. Ndipo watakutikisia vichwa vyao na watasema: Yatakuwa lini hayo? Sema: Huenda yakawa karibu.

يَوْمَ يَدْعُوْكُمْ فَتَسْتَجِيْبُوْنَ بِحَمْدِهٖ
وَتَظُنُّوْنَ اِنْ لَّبِثْتُمْ اِلَّا قَلِيْلًا ﴿٥٢﴾

53. Siku Atakapowaiteni, na ninyi mtaitika kwa kumsifu na mtafahamu kuwa hamkukaa (duniani) ila kidogo tu.

Aya 46. *Pazia* iliyotajwa hapa ni pazia ambayo baadhi ya wakati inakuwa ya kijicho na husuda; wakati mwingine inakuwa ya kujiona mkubwa na fahari ya kabila; wakati mwingine ni kuogopa kudharauliwa na watu na kupata hasara ya mali; au tena ni pazia ya mila na itikadi zinazopendelewa zilizokaa kwa muda mrefu, ambazo zinakingama katika njia ya wasioamini, wakazuilika kuikubali haki n.k.w. Ni pazia iliyofichikana ambayo wasioamini wenyewe hawaioni waziwazi.

FUNGU 6

وَقُلْ لِّعِبَادِيْ يَقُوْلُوا الَّتِيْ هِيَ اَحْسَنُ ؕ
اِنَّ الشَّيْطٰنَ يَنْزَغُ بَيْنَهُمْ ؕ اِنَّ الشَّيْطٰنَ
كَانَ لِلْاِنْسَانِ عَدُوًّا مُّبِيْنًا ﴿٥٣﴾

54. Na uwaambie watumishi wangu waseme yaliyo bora; maana Shetani huchochea magomvi kati yao. Hakika Shetani kwa mwanadamu ni adui dhahiri.

رَبُّكُمْ اَعْلَمُ بِكُمْ ؕ اِنْ يَّشَاْ يَرْحَمْكُمْ اَوْ
اِنْ يَّشَاْ يُعَذِّبْكُمْ ؕ وَمَآ اَرْسَلْنٰكَ عَلَيْهِمْ
وَكِيْلًا ﴿٥٤﴾

55. Mola wenu Anawajueni sana. Akipenda Atawarehemuni, au Akipenda Atawaadhibuni. Na Hatukukutuma kuwa mlinzi juu yao.

وَرَبُّكَ اَعْلَمُ بِمَنْ فِي السَّمٰوٰتِ
وَالْاَرْضِ ؕ وَلَقَدْ فَضَّلْنَا بَعْضَ النَّبِيّٖنَ
عَلٰى بَعْضٍ وَّاٰتَيْنَا دَاوٗدَ زَبُوْرًا ﴿٥٥﴾

56. Na Mola wako Anawajua sana wote waliomo katika mbingu na ardhi. Na kwa hakika Tuliwafadhili baadhi ya Manabii kuliko wengine; na Daudi Tulimpa Zaburi.

قُلِ ادْعُوا الَّذِيْنَ زَعَمْتُمْ مِّنْ دُوْنِهٖ فَلَا
يَمْلِكُوْنَ كَشْفَ الضُّرِّ عَنْكُمْ وَلَا
تَحْوِيْلًا ﴿٥٦﴾

57. Sema: Waiteni wale mnaowadai (kuwa waungu) badala Yake; kisha hawataweza kuwaondoleeni dhara wala kubadilisha.

اُولٰٓئِكَ الَّذِيْنَ يَدْعُوْنَ يَبْتَغُوْنَ اِلٰى
رَبِّهِمُ الْوَسِيْلَةَ اَيُّهُمْ اَقْرَبُ وَيَرْجُوْنَ
رَحْمَتَهٗ وَيَخَافُوْنَ عَذَابَهٗ ؕ اِنَّ عَذَابَ
رَبِّكَ كَانَ مَحْذُوْرًا ﴿٥٧﴾

58. Hao wanaowaita, (wenyewe) wanatafuta ukaribiano na Mola wao - (hata) aliye karibu sana miongoni mwao - na wanatumai rehema Zake, na wanaogopa adhabu Yake. Hakika adhabu ya Mola wako ni ya kuogopwa.

وَاِنْ مِّنْ قَرْيَةٍ اِلَّا نَحْنُ مُهْلِكُوْهَا قَبْلَ
يَوْمِ الْقِيٰمَةِ اَوْ مُعَذِّبُوْهَا عَذَابًا شَدِيْدًا ؕ
كَانَ ذٰلِكَ فِي الْكِتٰبِ مَسْطُوْرًا ﴿٥٨﴾

59. Na hakutakuwa mji ila Sisi Tutauhilikisha kabla ya siku ya Kiyama au kuuadhibu adhabu kali. Hayo yameandikwa katika Kitabu.

وَمَا مَنَعَنَآ اَنْ نُّرْسِلَ بِالْاٰيٰتِ اِلَّآ اَنْ
كَذَّبَ بِهَا الْاَوَّلُوْنَ ؕ وَاٰتَيْنَا ثَمُوْدَ النَّاقَةَ

60. Na hakuna kingetuzuia kuzipeleka Ishara ila ya kwamba watu wa zamani walizikadhibisha. Na Tuliwapa

Aya 56. *Zaburi* ina maana ya ngozi za ndama zilizotayarishwa kwa ajili ya maandishi.

Aya 60. *Hatuzipeleki Ishara ila kwa kuhadharisha.* Padre Dale alifurahishwa na wazo la kuikadhibisha Aya hii ya Qur'an. Anaandika, "Miujiza ya Bwana wetu ilikuwa miujiza ya rehema, huruma na upendo" (uk. 625 wa Tafsiri yake). Hata sisi tunasadiki kuwa Yesu alionyesha miujiza

مُبْصِرَةً فَظَلَمُوْا بِهَا ۭ وَمَا نُرْسِلُ
بِالْاٰيٰتِ اِلَّا تَخْوِيْفًا ۝٥٩

Wathamudi ngamia jike kuwa Ishara dhahiri, lakini wakamdhulumu. Na Hatuzipeleki Ishara ila kwa kuhadharisha.

وَاِذْ قُلْنَا لَكَ اِنَّ رَبَّكَ اَحَاطَ بِالنَّاسِ ۭ
وَمَا جَعَلْنَا الرُّءْيَا الَّتِيْٓ اَرَيْنٰكَ اِلَّا فِتْنَةً
لِّلنَّاسِ وَالشَّجَرَةَ الْمَلْعُوْنَةَ فِي الْقُرْاٰنِ ۭ
وَنُخَوِّفُهُمْ ۙ فَمَا يَزِيْدُهُمْ اِلَّا طُغْيَانًا
كَبِيْرًا ۝٦٠ ع

61. Na (kumbuka) Tulipokuambia: Hakika Mola wako Amewazunguka watu. Na Hatukuifanya njozi ile Tuliyokuonyesha ila kwa kuwajaribu watu, na (pia) mti uliolaaniwa katika Qur'an. Na Tunawahadharisha, lakini haiwazidishii ila uasi mkubwa.

FUNGU 7

وَاِذْ قُلْنَا لِلْمَلٰۗىِٕكَةِ اسْجُدُوْا لِاٰدَمَ
فَسَجَدُوْٓا اِلَّآ اِبْلِيْسَ ۭ قَالَ ءَاَسْجُدُ لِمَنْ
خَلَقْتَ طِيْنًا ۝٦١

62. Na (kumbuka) Tulipowaambia Malaika: Mtiini Adamu, basi wakamtii isipokuwa Ibilisi. Akasema: Je, nimtii yule Uliyemwumba kwa udongo.

قَالَ اَرَءَيْتَكَ هٰذَا الَّذِيْ كَرَّمْتَ عَلَيَّ ۡ
لَىِٕنْ اَخَّرْتَنِ اِلٰى يَوْمِ الْقِيٰمَةِ لَاَحْتَنِكَنَّ
ذُرِّيَّتَهٗٓ اِلَّا قَلِيْلًا ۝٦٢

63. Akasema: Unaonaje, huyu ndiye Umempa heshima zaidi kuliko mimi? Kama Ukinipa muda mpaka siku ya Kiyama, bila shaka nitawashika wazao wake ila wachache.

قَالَ اذْهَبْ فَمَنْ تَبِعَكَ مِنْهُمْ فَاِنَّ
جَهَنَّمَ جَزَاۗؤُكُمْ جَزَاۗءً مَّوْفُوْرًا ۝٦٣

64. (Allah) Akasema: Ondoka! Na atakayekufuata miongoni mwao, basi hakika Jahanamu ndiyo malipo yenu, malipo kamili.

وَاسْتَفْزِزْ مَنِ اسْتَطَعْتَ مِنْهُمْ
بِصَوْتِكَ وَاَجْلِبْ عَلَيْهِمْ بِخَيْلِكَ
وَرَجِلِكَ وَشَارِكْهُمْ فِي الْاَمْوَالِ

65. Na uwavute uwezao miongoni mwao kwa sauti yako, na uwakusanyie wapandao farasi wako, na waendao kwa

ya huruma na upendo. Mwujiza wake wa kwanza tu ulikuwa kutengeneza pombe nyingi arusini (Yohana 2:1-11). Huo ndiyo mwujiza wa upendo. Mwujiza wa huruma na rehema ulionekana alipotoa pepo (mizuka) wachafu katika mtu mmoja na akawatuma pepo hao katika kundi kubwa la nguruwe. "Wale pepo wachafu wakatoka, wakaingia katika wale nguruwe; nalo kundi lote likatelemka kwa kasi gengeni, wakaingia baharini, wapata elfu mbili; wakafa baharini" (Marko 5:13). Mtu ambaye nguruwe zake elfu mbili walizamishwa bure baharini kweli kweli aliona ameshukiwa na rehema nyingi za 'Bwana.' Labda ni kwa sababu hii watu wa huko "Wakaanza kumsihi aondoke mipakani mwao" (Marko 5"17).

Aya 61. *Njozi.* Neno njozi hapa mradi wake ni ile njozi ya *Israa* aliyoona Mtume *s.a.w.* ambayo tumeeleza habari zake mwanzo wa sura hii. Bibi Aisha alisema, "Mtume *s.a.w.* kiwiliwili chake hakikupotea bali alifanyiwa *Israa* kwa roho tu" (Ibni Is'hak).

miguu wako, na ushirikiane nao katika mali na watoto na uwaahidi. Lakini Shetani hawaahidi ila udanganyifu.

وَالْاَوْلَادِ وَعِدْهُمْ ؕ وَمَا يَعِدُهُمُ الشَّيْطٰنُ اِلَّا غُرُوْرًا ﴿٦٤﴾

66. Hakika watumishi Wangu huna mamlaka juu yao. Na Mola wako Anatosha kuwa Mlinzi.

اِنَّ عِبَادِيْ لَيْسَ لَكَ عَلَيْهِمْ سُلْطٰنٌ ؕ وَكَفٰى بِرَبِّكَ وَكِيْلًا ﴿٦٥﴾

67. Mola wenu ndiye Anayewaendesheeni merikebu katika bahari ili mtafute fadhili Zake. Bila shaka Yeye ni Mrehemevu kwenu

رَبُّكُمُ الَّذِيْ يُزْجِيْ لَكُمُ الْفُلْكَ فِي الْبَحْرِ لِتَبْتَغُوْا مِنْ فَضْلِهٖ ؕ اِنَّهٗ كَانَ بِكُمْ رَحِيْمًا ﴿٦٦﴾

68. Na inapowafikieni taabu katika bahari, hupotea wale mnaowaita isipokuwa Yeye tu. Lakini Anapowafikisheni salama nchi kavu, mnakengeuka; na mwanadamu ndiye akufuruye sana.

وَاِذَا مَسَّكُمُ الضُّرُّ فِي الْبَحْرِ ضَلَّ مَنْ تَدْعُوْنَ اِلَّآ اِيَّاهُ ۚ فَلَمَّا نَجّٰىكُمْ اِلَى الْبَرِّ اَعْرَضْتُمْ ؕ وَكَانَ الْاِنْسَانُ كَفُوْرًا ﴿٦٧﴾

69. Je, mmesalimika ya kuwa Hatawadidimizeni upande wa nchi-kavu au kuwapelekeeni tufani ya mchanga, kisha msipate mlinzi?

اَفَاَمِنْتُمْ اَنْ يَّخْسِفَ بِكُمْ جَانِبَ الْبَرِّ اَوْ يُرْسِلَ عَلَيْكُمْ حَاصِبًا ثُمَّ لَا تَجِدُوْا لَكُمْ وَكِيْلًا ﴿٦٨﴾

70. Au mmesalimika ya kuwa Hatawarudisheni humo (baharini) mara ya pili na kuwapelekeeni upepo mkali, na Awazamisheni kwa sababu mmekufuru; kisha hamtapata msaidizi juu Yetu kwa (adhabu) hii.

اَمْ اَمِنْتُمْ اَنْ يُّعِيْدَكُمْ فِيْهِ تَارَةً اُخْرٰى فَيُرْسِلَ عَلَيْكُمْ قَاصِفًا مِّنَ الرِّيْحِ فَيُغْرِقَكُمْ بِمَا كَفَرْتُمْ ۙ ثُمَّ لَا تَجِدُوْا لَكُمْ عَلَيْنَا بِهٖ تَبِيْعًا ﴿٦٩﴾

71. Na hakika Tumewaheshimu wanadamu na Tumewabeba barani na baharini, na Tumewaruzuku katika vitu vizuri, na Tumewatukuza kuliko wengi wa wale Tuliowaumba, kwa utukufu mkubwa.

وَلَقَدْ كَرَّمْنَا بَنِيْٓ اٰدَمَ وَحَمَلْنٰهُمْ فِي الْبَرِّ وَالْبَحْرِ وَرَزَقْنٰهُمْ مِّنَ الطَّيِّبٰتِ وَفَضَّلْنٰهُمْ عَلٰى كَثِيْرٍ مِّمَّنْ خَلَقْنَا تَفْضِيْلًا ﴿٧٠﴾ ع ۷

FUNGU 8

72. Siku Tutakapowaita kila watu pamoja na viongozi wao; basi atakayepewa daftari yake kwa mkono wake wa kulia, hao watasoma kitabu cha amali zao, wala hawatadhulumiwa hata kidogo.

يَوْمَ نَدْعُوْا كُلَّ اُنَاسٍۢ بِاِمَامِهِمْ ۚ فَمَنْ اُوْتِيَ كِتٰبَهٗ بِيَمِيْنِهٖ فَاُولٰٓئِكَ يَقْرَءُوْنَ كِتٰبَهُمْ وَلَا يُظْلَمُوْنَ فَتِيْلًا ﴿٧١﴾

73. Na aliye kipofu katika (dunia) hii, basi atakuwa kipofu katika Akhera, na Atakuwa aliyeipotea zaidi njia.

وَمَنْ كَانَ فِيْ هٰذِهٖۤ اَعْمٰى فَهُوَ فِى الْاٰخِرَةِ اَعْمٰى وَاَضَلُّ سَبِيْلًا ﴿٧٢﴾

74. Na hakika walikuwa karibu kukuadhibu kwa sababu ya yale Tuliyokufunulia ili upate kututungia badala ya haya; na hapo bila shaka wangalikufanya rafiki mkubwa.

وَاِنْ كَادُوْا لَيَفْتِنُوْنَكَ عَنِ الَّذِىْۤ اَوْحَيْنَاۤ اِلَيْكَ لِتَفْتَرِىَ عَلَيْنَا غَيْرَهٗ ۖ وَاِذًا لَّاتَّخَذُوْكَ خَلِيْلًا ﴿٧٣﴾

75. Na kama Tusingalikuimarisha (kwa Qur'an hii) kwa yakini ungalikuwa karibu kuwaelekea kidogo.

وَلَوْلَاۤ اَنْ ثَبَّتْنٰكَ لَقَدْ كِدْتَّ تَرْكَنُ اِلَيْهِمْ شَيْـًٔا قَلِيْلًا ﴿٧٤﴾

76. Hapo bila shaka Tungalikuonjesha adhabu kubwa ya maisha na adhabu kubwa ya mauti; kisha usingepata msaidizi dhidi Yetu.

اِذًا لَّاَذَقْنٰكَ ضِعْفَ الْحَيٰوةِ وَضِعْفَ الْمَمَاتِ ثُمَّ لَا تَجِدُ لَكَ عَلَيْنَا نَصِيْرًا ﴿٧٥﴾

77. Na kwa hakika wako karibu kukufukuza katika nchi ili wakutoe humo; na ndipo wasingalikaa nyuma yako ila (muda) kidogo tu.

وَاِنْ كَادُوْا لَيَسْتَفِزُّوْنَكَ مِنَ الْاَرْضِ لِيُخْرِجُوْكَ مِنْهَا وَاِذًا لَّا يَلْبَثُوْنَ خِلٰفَكَ اِلَّا قَلِيْلًا ﴿٧٦﴾

78. Ndiyo desturi ya wale Tuliowatuma kabla yako katika Mitume Wetu; wala hutapata mabadiliko katika desturi Yetu.

سُنَّةَ مَنْ قَدْ اَرْسَلْنَا قَبْلَكَ مِنْ رُّسُلِنَا وَلَا تَجِدُ لِسُنَّتِنَا تَحْوِيْلًا ﴿٧٧﴾ ع ٨

FUNGU 9

79. Usimamishe Sala jua linapopinduka mpaka giza la usiku, na kusoma Qur'an alfajiri. Hakika kusoma Qur'an alfajiri kunakubaliwa (sana).

اَقِمِ الصَّلٰوةَ لِدُلُوْكِ الشَّمْسِ اِلٰى غَسَقِ الَّيْلِ وَقُرْاٰنَ الْفَجْرِ ؕ اِنَّ قُرْاٰنَ الْفَجْرِ كَانَ مَشْهُوْدًا ﴿٧٨﴾

Aya 73. Aya hii inaeleza ya kwamba watu wasiotumia vema macho yao ya kiroho katika maisha haya, watayalemaza, hata katika Akhera watajiona wamefufuka vipofu. Qur'an imewaita" vipofu" watu wasiofikiria Ishara za Allah.

Aya 79. *Duluuki-sh-shams.* Tamko hili lina maana tatu: (a) Jua linapopinduka; (b) Jua linapokuwa rangi ya manjano; na (c) Jua linapotua (Akrab).

Maneno ya Aya hii yanaonyesha nyakati tano za Sala. Neno *duluuk* linaonyesha nyakati za Sala za Adhuhuri na Alasiri na Magharibi. Maneno *ghasaqillail* yanakusanya nyakati za Sala ya Magharibi, lakini hasa Sala ya Isha. Na *Qur'aanul-fajr* (kusoma Qur'an alfajiri) yanaonyesha Sala ya Alfajiri.

وَمِنَ الَّيْلِ فَتَهَجَّدْ بِهٖ نَافِلَةً لَّكَ ۖ عَسٰٓى
اَنْ يَّبْعَثَكَ رَبُّكَ مَقَامًا مَّحْمُوْدًا ﴿٧٩﴾

80. Na katika usiku, pia amka (uisome): ndiyo ibada zaidi kwako. Huenda Mola wako Akakuinua cheo kinachosifika.

وَقُلْ رَّبِّ اَدْخِلْنِيْ مُدْخَلَ صِدْقٍ
وَّاَخْرِجْنِيْ مُخْرَجَ صِدْقٍ وَّاجْعَلْ
لِّيْ مِنْ لَّدُنْكَ سُلْطٰنًا نَّصِيْرًا ﴿٨٠﴾

81. Na sema: Mola wangu Uniingize mwingizo mwema, na Unitoe kutoka kwema. Na Unipe nguvu kutoka Kwako isaidiayo.

وَقُلْ جَآءَ الْحَقُّ وَزَهَقَ الْبَاطِلُ ۭ اِنَّ
الْبَاطِلَ كَانَ زَهُوْقًا ﴿٨١﴾

82. Na sema: Ukweli umefika na uwongo umetoweka; hakika uwongo ndiyo wenye kutoweka.

وَنُنَزِّلُ مِنَ الْقُرْاٰنِ مَا هُوَ شِفَاۗءٌ وَّرَحْمَةٌ
لِّلْمُؤْمِنِيْنَ ۙ وَلَا يَزِيْدُ الظّٰلِمِيْنَ اِلَّا
خَسَارًا ﴿٨٢﴾

83. Na Tunateremsha pole pole katika Qur'an (mafundisho) ambayo ni ponyo na rehema kwa waaminio; wala hayawazidishii wadhalimu ila hasara tu.

وَاِذَآ اَنْعَمْنَا عَلَي الْاِنْسَانِ اَعْرَضَ
وَنَاٰ بِجَانِبِهٖ ۚ وَاِذَا مَسَّهُ الشَّرُّ كَانَ
يَـُٔوْسًا ﴿٨٣﴾

84. Na Tunapomneemesha mwanadamu, hukengeuka na kuenda upande; na inapomgusa shari hukata tamaa.

قُلْ كُلٌّ يَّعْمَلُ عَلٰي شَاكِلَتِهٖ ۭ فَرَبُّكُمْ
اَعْلَمُ بِمَنْ هُوَ اَهْدٰى سَبِيْلًا ﴿٨٤﴾ ع

85. Sema: Kila mmoja hufanya kwa njia yake, na Mola wenu Anamjua sana aliyeongoka zaidi katika njia.

Habari za nyakati za Sala pia zimeelezwa katika sura hizi: 11:115; 20:131; 30:18-19 na 50:40.

Mtume *s.a.w.* alilinganisha Sala tano na mto wa maji unaopita mbele ya nyumba ya mtu, naye akikoga humo mara tano kutwa, hawezi kubakiwa na uchafu mwilini mwake. Akasema kuwa Sala tano ni kama hivyo, humfutia mtu madhambi yake yote (Bukhari).

Aya 80. *Amka uisome. Tahajjud* ni kuamka baada ya kulala. Mtume *s.a.w.* alikuwa analala katika sehemu ya kwanza ya usiku na katika sehemu ya mwisho ya usiku alikuwa anaamka na kushughulika katika ibada na kusoma Qur'an sana katika Sala. Hivyo, katika matamko ya Kiislamu, Sala hii ya sehemu ya mwisho wa usiku imeitwa Sala ya Tahajjud.

Ndiyo (ibada) zaidi kwako. Maneno haya yanajulisha ya kuwa ibada hii ni neema hasa na zawadi itokayo kwa Allah ambayo humfikisha mtu kwenye cheo kikubwa cha heshima sana kilichotajwa juu.

Kwa hakika katika Aya hizi mbili zimeelezwa namna mbili za Sala. (a) Sala zilizo faradhi, yaani Sala tano; (b) Sala zilizo Nafl - kama Sala ya Tahajjud. Na kwa kutaja Sala hizi za namna mbili, Allah amewahimiza Waislamu ya kuwa kwa kupata ushindi na ufaulu juu ya maadui, waelekee kwa Allah na washike ibada, ndipo fitina zitaondoka na maadui hawatafaulu. Tunaona katika maisha ya Mtume wetu Muhammad *s.a.w.,* waliokuwa maadui kama Ilkrima bin Abu Jahal, Khalid bin Walid, 'Amar bin al-A'as na wanawake maadui kama Hindi bint Abu Sufyan, wakawa waaminio halisi na wakampenda sana Mtume *s.a.w.* Hawa wote walivutwa na dua na ibada za Mtume *s.a.w.*

FUNGU 10

وَ يَسْـَٔلُوْنَكَ عَنِ الرُّوْحِ ؕ قُلِ الرُّوْحُ مِنْ اَمْرِ رَبِّیْ وَمَاۤ اُوْتِیْتُمْ مِّنَ الْعِلْمِ اِلَّا قَلِیْلًا ﴿۸۵﴾

86. Na wanakuuliza juu ya roho. Sema: Roho imetokana na amri ya Mola wangu; nanyi hamkupewa katika elimu (ya roho) ila kidogo.

وَلَئِنْ شِئْنَا لَنَذْهَبَنَّ بِالَّذِیْۤ اَوْحَیْنَاۤ اِلَیْكَ ثُمَّ لَا تَجِدُ لَكَ بِهٖ عَلَیْنَا وَكِیْلًا ﴿۸۶﴾

87. Na kama Tungalipenda, bila shaka Tungaliondoa yale Tuliyokufunulia, kisha usingalipata kwa (jambo) hili mlinzi juu Yetu;

اِلَّا رَحْمَةً مِّنْ رَّبِّكَ ؕ اِنَّ فَضْلَهٗ كَانَ عَلَیْكَ كَبِیْرًا ﴿۸۷﴾

88. Ila rehema itokayo kwa Mola wako. Hakika fadhili yake iliyo juu yako ni kubwa.

قُلْ لَّئِنِ اجْتَمَعَتِ الْاِنْسُ وَالْجِنُّ عَلٰۤی اَنْ یَّاْتُوْا بِمِثْلِ هٰذَا الْقُرْاٰنِ لَا یَاْتُوْنَ بِمِثْلِهٖ وَلَوْ كَانَ بَعْضُهُمْ لِبَعْضٍ ظَهِیْرًا ﴿۸۸﴾

89. Sema: Kama wajikusanye watu na majini kwa kuleta mfano wa Qur'an hii, hawataweza kuleta mfano wake hata kama wasaidiane wao kwa wao.

وَلَقَدْ صَرَّفْنَا لِلنَّاسِ فِیْ هٰذَا الْقُرْاٰنِ مِنْ كُلِّ مَثَلٍ ۬ فَاَبٰۤی اَكْثَرُ النَّاسِ اِلَّا كُفُوْرًا ﴿۸۹﴾

90. Na bila shaka Tumewaeleza watu kwa namna nyingi katika Qur'an hii kila mfano, lakini watu wengi zaidi wakakataa (kila kitu) isipokuwa kufuru.

وَقَالُوْا لَنْ نُّؤْمِنَ لَكَ حَتّٰی تَفْجُرَ لَنَا مِنَ الْاَرْضِ یَنْۢبُوْعًا ﴿۹۰﴾

91. Na wakasema: Hatuwezi kukuamini mpaka utububujishie chemchem katika ardhi.

اَوْ تَكُوْنَ لَكَ جَنَّةٌ مِّنْ نَّخِیْلٍ وَّعِنَبٍ فَتُفَجِّرَ الْاَنْهٰرَ خِلٰلَهَا تَفْجِیْرًا ﴿۹۱﴾

92. Au uwe na bustani ya mitende na mizabibu, kisha ukabubujishe mito katikati yake kwa mbubujiko.

اَوْ تُسْقِطَ السَّمَآءَ كَمَا زَعَمْتَ عَلَیْنَا كِسَفًا اَوْ تَاْتِیَ بِاللّٰهِ وَالْمَلٰٓئِكَةِ قَبِیْلًا ﴿۹۲﴾

93. Au utuangushie mbingu vipande-vipande kama ulivyodai, au utuletee Allah na Malaika ana kwa ana.

Aya 86. Baadhi ya madhehebu ya Kibaniani na wengineo wanasadiki ya kuwa roho si kiumbe cha Mungu, bali ni kitu kilichokuwapo tangu na tangu kama vile alivyokuwapo Allah Mwenyewe. Katika Aya hii Allah anavunja madai yao hayo na anasema ya kuwa roho imetokana na amri Yake, yaani imeumbwa. Kuumba ni namna mbili. Namna moja ni *khalq* yaani kitu kinaumbwa toka kitu kingine, kama alivyoumbwa mtu na vitu vingine. Namna ya pili ya kuumba ni kwa *amr*, yaani kitu kinaumbwa pasipokuwa kitu. Na roho ni kiumbe cha namna hii ya pili.

94. Au uwe na nyumba ya dhahabu, au upande mbinguni; na hatutaamini kupanda kwako mpaka ututeremshie kitabu tukisome. Sema: Mola wangu ni Mtakatifu! mimi siye ila ni mtu tu, Mtume.

اَوْ يَكُوْنَ لَكَ بَيْتٌ مِّنْ زُخْرُفٍ اَوْ
تَرْقٰى فِي السَّمَآءِ ؕ وَلَنْ نُّؤْمِنَ لِرُقِيِّكَ
حَتّٰى تُنَزِّلَ عَلَيْنَا كِتٰبًا نَّقْرَؤُهٗ ؕ
قُلْ سُبْحَانَ رَبِّيْ هَلْ كُنْتُ اِلَّا
بَشَرًا رَّسُوْلًا ﴿٩٤﴾ ع

FUNGU 11

95. Na hapana lililowakataza watu kuamini ulipowafikia mwongozo, isipokuwa walisema: Je, Allah Amemtuma mtu kuwa Mtume?

وَمَا مَنَعَ النَّاسَ اَنْ يُّؤْمِنُوْٓا اِذْ جَآءَهُمُ
الْهُدٰٓى اِلَّآ اَنْ قَالُوْٓا اَبَعَثَ اللّٰهُ
بَشَرًا رَّسُوْلًا ﴿٩٥﴾

96. Sema: Kama katika ardhi wangalikuwa Malaika watembeao kwa utulivu, bila shaka Tungaliwateremshia kutoka mbinguni Malaika Mtume.

قُلْ لَّوْ كَانَ فِي الْاَرْضِ مَلٰٓئِكَةٌ يَّمْشُوْنَ
مُطْمَئِنِّيْنَ لَنَزَّلْنَا عَلَيْهِمْ مِّنَ السَّمَآءِ
مَلَكًا رَّسُوْلًا ﴿٩٦﴾

97. Sema: Allah Anatosha kuwa Shahidi baina yangu na baina yenu; hakika Yeye kwa watumishi Wake ni Ajuaye, Aonaye.

قُلْ كَفٰى بِاللّٰهِ شَهِيْدًا ۢ بَيْنِيْ وَبَيْنَكُمْ ؕ
اِنَّهٗ كَانَ بِعِبَادِهٖ خَبِيْرًا ۢ بَصِيْرًا ﴿٩٧﴾

98. Na ambaye Allah Anamwongoza, basi yeye ndiye aliyeongoka; na Anayemwangamiza, basi wewe hutawapatia walinzi ghairi Yake. Na Tutawakusanya siku ya Kiyama juu ya nyuso zao katika hali ya upofu na ububu na uziwi. Makao yao ni Jahanamu; kila izimikapo kidogo Tutawazidishia mwako.

وَمَنْ يَّهْدِ اللّٰهُ فَهُوَ الْمُهْتَدِ ۚ وَمَنْ يُّضْلِلْ
فَلَنْ تَجِدَ لَهُمْ اَوْلِيَآءَ مِنْ دُوْنِهٖ ؕ
وَنَحْشُرُهُمْ يَوْمَ الْقِيٰمَةِ عَلٰى وُجُوْهِهِمْ
عُمْيًا وَّبُكْمًا وَّصُمًّا ؕ مَاْوٰىهُمْ جَهَنَّمُ ؕ
كُلَّمَا خَبَتْ زِدْنٰهُمْ سَعِيْرًا ﴿٩٨﴾ ع

Aya 94. Makafiri waliposikia habari za Mi'raaj walimwambia Mtume *s.a.w.* ya kuwa hawawezi kukubali kuwa kweli alikwenda mbinguni mpaka apande mbinguni mbele ya macho yao, na awateremshie Kitabu. Mtume *s.a.w.* aliambiwa na Allah kuwajibu ya kuwa Mungu ni Mtakatifu, na yeye Mtume ni mwanadamu tu; yaani si kazi ya Mungu kuonyesha tamasha za namna hiyo, wala si shani ya mwanadamu kupanda mbinguni na kiwiliwili chake. Ingekuwa desturi ya wanadamu walio Manabii kupanda mbinguni na viwiliwili vyao, kama wasemavyo baadhi ya watu ya kuwa Nabii Isa amepanda mbinguni, basi Mtume wetu Muhammad *s.a.w.* angepokea mara moja ombi la makafiri. Lakini kwa kuwajibu kama vile alivyowajibu, inaonekana wazi kabisa kuwa kupaa mbinguni na mwili wa kidunia ni desturi isiyojulikana kwa Manabii wala siyo njia ya kuhakikisha ukweli wao.

ذٰلِكَ جَزَآؤُهُمْ بِاَنَّهُمْ كَفَرُوْا بِاٰيٰتِنَا وَقَالُوْٓا ءَاِذَا كُنَّا عِظَامًا وَّرُفَاتًا ءَاِنَّا لَمَبْعُوْثُوْنَ خَلْقًا جَدِيْدًا ﴿٩٩﴾

99. Hayo ni malipo yao kwa sababu walizikataa Ishara Zetu na wakasema: Je, Tutakapokuwa mifupa na chembe zilizosagika, je, tutafufuliwa kuwa viumbe wapya?

اَوَلَمْ يَرَوْا اَنَّ اللّٰهَ الَّذِيْ خَلَقَ السَّمٰوٰتِ وَالْاَرْضَ قَادِرٌ عَلٰٓى اَنْ يَّخْلُقَ مِثْلَهُمْ وَجَعَلَ لَهُمْ اَجَلًا لَّا رَيْبَ فِيْهِ ؕ فَاَبَى الظّٰلِمُوْنَ اِلَّا كُفُوْرًا ﴿١٠٠﴾

100, Je, hawakuona ya kwamba Allah Aliyeziumba mbingu na ardhi ni Mwenye uwezo wa kuumba mfano wa wao? Na Amewawekea muda usiyo na shaka. Lakini wadhalimu wamekataa (kila kitu) isipokuwa kukufuru.

قُلْ لَّوْ اَنْتُمْ تَمْلِكُوْنَ خَزَآئِنَ رَحْمَةِ رَبِّيْٓ اِذًا لَّاَمْسَكْتُمْ خَشْيَةَ الْاِنْفَاقِ ؕ وَكَانَ الْاِنْسَانُ قَتُوْرًا ﴿١٠١﴾ ع

101. Sema: Kama mngalizimiliki hazina za rehema ya Mola wangu, ndipo bila shaka ninyi mngalizizuia kwa kuogopa kuzitumia; na mwanadamu ni mchoyo sana.

FUNGU 12

وَلَقَدْ اٰتَيْنَا مُوْسٰى تِسْعَ اٰيٰتٍۢ بَيِّنٰتٍ فَسْـَٔلْ بَنِيْٓ اِسْرَآءِيْلَ اِذْ جَآءَهُمْ فَقَالَ لَهٗ فِرْعَوْنُ اِنِّيْ لَاَظُنُّكَ يٰمُوْسٰى مَسْحُوْرًا ﴿١٠٢﴾

102. Na kwa yakini Tulimpa Musa Ishara tisa zilizo wazi; basi waulize wana wa Israeli alipowafikia, na Firauni akamwambia: Hakika mimi nakuona, Ewe Musa, umelogwa.

قَالَ لَقَدْ عَلِمْتَ مَآ اَنْزَلَ هٰٓؤُلَآءِ اِلَّا رَبُّ السَّمٰوٰتِ وَالْاَرْضِ بَصَآئِرَ ۚ وَاِنِّيْ لَاَظُنُّكَ يٰفِرْعَوْنُ مَثْبُوْرًا ﴿١٠٣﴾

103. Akasema: Bila shaka umekwisha jua hakuna aliyeteremsha (Ishara) hizi isipokuwa Mola wa mbingu na ardhi, kuwa dalili; na hakika mimi nakuona, Ewe Firauni, umekwisha angamia.

Aya 99. Sababu yote ya kukosa kuamini asili yake ni kutoiamini Akhera. Hii ndiyo sababu Qur'an imetia mkazo sana juu ya maisha yanayokuja baada ya kufa, na inarejea mara kwa mara kueleza jambo hili.

Aya 102. Ishara tisa zinazosemwa hapa zimetajwa kwa mgusio tu mahali pengine katika Qur'an. Ishara hizo ni hizi: (1) fimbo (sura 7:108); (2) mkono mweupe (sura 7:109); (3), (4)

فَاَرَادَ اَنۡ يَّسۡتَفِزَّهُمۡ مِّنَ الۡاَرۡضِ فَاَغۡرَقۡنٰهُ وَمَنۡ مَّعَهٗ جَمِيۡعًا ﴿۱۰۴﴾

104. Basi (Firauni) akataka kuwafukuza katika nchi; kwa hiyo Tukamzamisha yeye na waliokuwa pamoja naye wote.

وَّقُلۡنَا مِنۡۢ بَعۡدِهٖ لِبَنِىۡۤ اِسۡرَآءِيۡلَ اسۡكُنُوا الۡاَرۡضَ فَاِذَا جَآءَ وَعۡدُ الۡاٰخِرَةِ جِئۡنَا بِكُمۡ لَفِيۡفًا ﴿۱۰۵﴾

105. Na baada yake tukawaambia wana wa Israeli, "Kaeni katika nchi;" na itakapofika ahadi ya siku za mwisho Tutawaleteni tena pamoja.

وَبِالۡحَقِّ اَنۡزَلۡنٰهُ وَبِالۡحَقِّ نَزَلَ ؕ وَمَاۤ اَرۡسَلۡنٰكَ اِلَّا مُبَشِّرًا وَّنَذِيۡرًا ﴿۱۰۶﴾ ع

106. Na kwa haki Tumeiteremsha (Qur'an), na kwa haki imeteremka. Na Hatukukutuma ila uwe Mtoaji wa habari njema na Mwonyaji.

وَقُرۡاٰنًا فَرَقۡنٰهُ لِتَقۡرَاَهٗ عَلَى النَّاسِ عَلٰى مُكۡثٍ وَّنَزَّلۡنٰهُ تَنۡزِيۡلًا ﴿۱۰۷﴾

107. Na Qur'an Tumeigawanya sehemu-sehemu ili uisome kwa watu kwa vituo, na Tumeiteremsha kidogo kidogo.

قُلۡ اٰمِنُوۡا بِهٖۤ اَوۡ لَا تُؤۡمِنُوۡا ؕ اِنَّ الَّذِيۡنَ اُوۡتُوا الۡعِلۡمَ مِنۡ قَبۡلِهٖۤ اِذَا يُتۡلٰى عَلَيۡهِمۡ يَخِرُّوۡنَ لِلۡاَذۡقَانِ سُجَّدًا ﴿۱۰۸﴾

108. Sema: Muiamini au msiiamini. Hakika wale waliopewa elimu kabla yake wanapoisomewa, huangukia nyuso kusujudu.

وَّيَقُوۡلُوۡنَ سُبۡحٰنَ رَبِّنَاۤ اِنۡ كَانَ وَعۡدُ رَبِّنَا لَمَفۡعُوۡلًا ﴿۱۰۹﴾

109. Na wanasema: Mola wetu ni Mtakatifu. Hakika ahadi ya Mola wetu ndiyo itimizwayo.

وَيَخِرُّوۡنَ لِلۡاَذۡقَانِ يَبۡكُوۡنَ وَيَزِيۡدُهُمۡ خُشُوۡعًا ﴿۱۱۰﴾ السجدة

110. Na huangukia nyuso wakilia, na inawazidishia unyenyekevu.

---

kukosa mvua na kupungua matunda kwa maana ya vifo vya watoto waliozaliwa kwanza (sura 7:131); (5) tufani; (6) nzige; (7) chawa; (8) vyura; na (9) adhabu ya damu (sura 7:134).

Aya 105. *Kaeni katika nchi,* yaani nchi ya Kanan.

Aya 106. *Hatukukutuma ila uwe Mtoaji wa habari njema na Mwonyaji.* Maneno haya ni bishara ya kuangamizwa maadui wa Uislamu na kushinda kwa Waislamu.

111. Sema: Mwiteni Allah au mwiteni Rahman; kwa jina lo lote ambalo kwalo mtamwomba, Yake ni majina mazuri. Wala usiseme sala yako kwa sauti kubwa wala usiseme kwa sauti ndogo bali tafuta njia iliyo baina ya hizo.

قُلِ ادْعُوا اللّٰهَ اَوِ ادْعُوا الرَّحْمٰنَ ؕ اَيًّا مَّا تَدْعُوْا فَلَهُ الْاَسْمَآءُ الْحُسْنٰى ۚ وَلَا تَجْهَرْ بِصَلَاتِكَ وَلَا تُخَافِتْ بِهَا وَابْتَغِ بَيْنَ ذٰلِكَ سَبِيْلًا ﴿١١١﴾

112. Na sema: Sifa zote njema zinamhusu Allah Ambaye Hakupanga mwana wala Hana mshirika katika ufalme, wala Hana rafiki kwa sababu ya udhaifu; na umtukuze kwa nguvu zote.

وَقُلِ الْحَمْدُ لِلّٰهِ الَّذِيْ لَمْ يَتَّخِذْ وَلَدًا وَّلَمْ يَكُنْ لَّهٗ شَرِيْكٌ فِي الْمُلْكِ وَلَمْ يَكُنْ لَّهٗ وَلِيٌّ مِّنَ الذُّلِّ وَكَبِّرْهُ تَكْبِيْرًا ﴿١١١﴾ ع ١٢

Aya 111. Aya hii inawafundisha waaminio kuwa wanapoomba cho chote kwa Allah wataje Majina au Sifa Zake zinazohusiana na maombi yao.

Aya 112. Aya hii inamaliza habari za *Israa* iliyotajwa mwanzoni kwa kubainisha kuwa bishara zilizotolewa na Israa hiyo zitahakikisha ushindi wa Uislamu na kushindwa ibada ya masanamu na kuvunjika itikadi za utatu wa Wakristo na waungu wengi. Basi mambo haya yaliyobashiriwa na Mtume *s.a.w.* yatapotimia itajulikana wazi ya kuwa Allah ndiye aliyemfunulia Mjumbe Wake bishara hizo, naye ni Mungu Mmoja wa kweli, ambaye hana mwana wala mshirika.

سُوْرَةُ الْكَهْفِ مَكِّيَّةٌ وَّ هِيَ مَعَ الْبَسْمَلَةِ مِائَةٌ وَّ اِحْدٰى عَشْرَةَ اٰيَةً وَّ اثْنَاعَشَرَ رُكُوْعًا

18. SURA AL-KAHF

Imeteremshwa Makka

Ina mafungu 12 na Aya 111 pamoja na Bismillahi

بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ ①

1. Kwa jina la Allah, Mwingi wa rehema, Mwingi wa ukarimu.

اَلْحَمْدُ لِلّٰهِ الَّذِيْٓ اَنْزَلَ عَلٰى عَبْدِهِ الْكِتٰبَ وَلَمْ يَجْعَلْ لَّهٗ عِوَجًا ؕ ②

2. Sifa zote njema zinamhusu Allah Ambaye amemteremshia Mtumishi wake Kitabu, na wala hakukifanyia tenge.

Ibni Abbas na Ibni Zubair wanasema ya kuwa sura hii yote ilishuka Makka (Manthur). Karibu wafasiri wote wa Qur'an wanakubaliana juu ya jambo hili. Anas anasimulia ya kwamba sura hii haikuteremshwa vipande vipande, bali ilishuka yote nzima na ilichungwa na Malaika 70,000 (sabini elfu) (Manthur, jalada 4, uk. 210).

Kwa kuwa sura hii ina bishara za kuangamizwa mataifa makubwa-makubwa ya *Yaajuj* na *Maajuj* na kuvunjika propaganda wanayoendesha Wakristo juu ya Uislamu, maelfu na maelfu ya Malaika wameshughulika kuleta matimizo ya bishara hizi zenye nguvu, toka siku sura hii ilipoteremka.

Heshima na nguvu ya mataifa ya Kikristo na umaskini na unyonge wa Waislamu vimeelezwa katika "mfano wa watu wawili" katika fungu la 5: mmoja tajiri na mwingine maskini. Mtu tajiri - mataifa ya Wakristo - atajivuna kwa utajiri wake, na maskini ataelekea kwa Allah. Kiburi na majivuno mwishoni vitaleta msiba na yatajitokeza mambo yasiyoweza kuzuiliwa na mwanadamu yatakayomwangusha tajiri.

Kisha Sura hii imeendelea kueleza mabadiliko makubwa aliyoonyeshwa Nabii Musa katika njozi yake inayoelezwa toka Fungu la tisa. Nabii Musa aliambiwa ya kwamba kukua na kuendelea kwa Sheria ya dini yake kutakuwa chini kabisa ya Sheria nyingine itakayofika baadaye. Hii Sheria ya dini ya baadaye itakamilisha mafundisho yaliyoachwa na dini ya Nabii Musa bila kukamilishwa; na dini ya Kiislamu itainuka yenye kushinda kutoka katika majivu ya kuzimika na kupooza kwa Ukristo.

Baada ya sura hii kueleza kuchakaa na kufa kwa dini ya Kikristo na kuinuka kwa Uislamu, inaendelea kueleza matukio yatakayokuja baada ya kufanikiwa Uislamu. Inaeleza ya kwamba utafika wakati Waislamu watakapoacha dini na wataelekea dunia. Ili kuwaadhibu, Allah atayapa tena mataifa ya Kikristo mafanikio na ustawi ingawa hapo kwanza yalizuiliwa kuingia nchi za Kusini na za Mashariki. Kisha mahilikisho makubwa yatatokea duniani, na mataifa yote yatagawanyika katika mafungu mawili yanayoaduiana, na yenye fikira mbili zinazopingana. Dhambi na uovu vitaenea duniani na dhuluma na jeuri vitatapakaa. Mambo yatakapofika kiasi hicho, Allah atatengeneza hali zitakazokomesha ghasia hizo zisizodhaniwa kuzuilika. Katika kueleza jambo hili,sura hii inagusia waziwazi ya kwamba, wale wale waliomzuia *Yaajuuj* na *Maajuuj* hapo kwanza ndio watakaozuia ghasia hizi za dunia, yaani wafuasi wa Mtume Muhammad *s.a.w.*

Aya 2. *'Iwajun.* Neno hili maana yake ni kombo; kota; upotofu; mpindo; mpindiko; kutokuwa sawa; uharibifu; upotevu; mageuzi; makosa n.k.w.

قَيِّمًا لِّيُنْذِرَ بَاْسًا شَدِيْدًا مِّنْ لَّدُنْهُ وَيُبَشِّرَ الْمُؤْمِنِيْنَ الَّذِيْنَ يَعْمَلُوْنَ الصّٰلِحٰتِ اَنَّ لَهُمْ اَجْرًا حَسَنًا ۙ﴿۳﴾

3. Kilinzi, ili kiwaonye watu adhabu kali itokayo Kwake, na kiwape habari njema waaminio ambao wanafanya vitendo vizuri ya kwamba watapata malipo mema.

مَّاكِثِيْنَ فِيْهِ اَبَدًا ۙ﴿۴﴾

4. Wakikaa humo milele.

وَّيُنْذِرَ الَّذِيْنَ قَالُوا اتَّخَذَ اللّٰهُ وَلَدًا ۗ﴿۵﴾

5. Na kiwaonye wale wanaosema: Allah Amepanga mwana.

مَا لَهُمْ بِهٖ مِنْ عِلْمٍ وَّلَا لِاٰبَآئِهِمْ ؕ كَبُرَتْ كَلِمَةً تَخْرُجُ مِنْ اَفْوَاهِهِمْ ؕ اِنْ يَّقُوْلُوْنَ اِلَّا كَذِبًا ﴿۶﴾

6. Wao hawana elimu ya jambo hili, wala baba zao. Ni neno kubwa litokalo katika vinywa vyao; hawasemi ila uwongo tu.

فَلَعَلَّكَ بَاخِعٌ نَّفْسَكَ عَلٰٓى اٰثَارِهِمْ اِنْ لَّمْ يُؤْمِنُوْا بِهٰذَا الْحَدِيْثِ اَسَفًا ﴿۷﴾

7. Basi huenda utajiangamiza nafsi yako kwa kusikitikia hali yao ikiwa hawaiamini hadithi hii.

اِنَّا جَعَلْنَا مَا عَلَى الْاَرْضِ زِيْنَةً لَّهَا لِنَبْلُوَهُمْ اَيُّهُمْ اَحْسَنُ عَمَلًا ﴿۸﴾

8. Kwa hakika Tumevifanya vilivyoko juu ya ardhi viwe mapambo yake, ili Tuwajaribu ni nani wao mwenye vitendo vizuri zaidi.

وَاِنَّا لَجٰعِلُوْنَ مَا عَلَيْهَا صَعِيْدًا جُرُزًا ؕ﴿۹﴾

9. Na hakika Sisi ni Wavifanyao vilivyoko juu yake kuwa ardhi kame.

اَمْ حَسِبْتَ اَنَّ اَصْحٰبَ الْكَهْفِ وَالرَّقِيْمِ ۙ كَانُوْا مِنْ اٰيٰتِنَا عَجَبًا ﴿۱۰﴾

10. Je, unafikiri ya kwamba watu wa Pango na Mwandiko walikuwa ajabu katika Ishara Zetu?

Kijina *huu* katika neno *lahuu* kinamhusu mtumishi wa Allah - mpokeaji wa Kitabu na vile linakihusu Kitabu chenyewe. Hivyo basi aya hii haiwezi kutafsiriwa kwa Kiswahili kwa kutumia kijina kimoja ambacho kitahusiana na Mtumishi na wakati huo huo kihusiane na Kitabu. Kama mtu aitafsiri kwamba: "Allah Hakuweka tenge ndani ya hicho kitabu", tafsiri hiyo haitakuwa imemjumuisha Mtukufu Mtume s.a.w. katika ahadi hii ya utakaso. Kama mtu aitafsiri kwamba "Hakuweka tenge nafsini mwa yeye", basi kitabu kitakuwa kimeachwa nje ya utakatifu huu. Ili kulitatua tatizo hili tumeitafsiri aya hii kwa mtindo tofauti wenye kuzingatia kikamilifu ile maana iliyokusudiwa kuliko kutilia mkazo zaidi kwenye herufi.

Aya 3. *Qayyiman.* Neno hili tumelifasiri "Kilinzi" na pia lina maana hizi nyingine: Kamilifu, chenye ukweli, kisimamizi (Lane, Akrab na Mufradat).

Aya 10. *As'haabul-Kahf warraqiim.* " Watu wa Pango na Mwandiko," ni wafuasi wa Nabii Isa. Watu wa Pango ni wafuasi wake wa zamani waliokataa kuabudu masanamu, na kwa kuogopa uadui wa wafalme wa kikafiri waliokuwa siku zile wakakimbilia pangoni, wakawa wanakaa huko. Na *Watu wa Mwandiko* ni hawa Wakristo wa leo ambao wameachana kabisa na

11. (Kumbukeni) baadhi ya vijana walipokimbilia kwenye pango na wakasema: Mola wetu, Utupe rehema kutoka Kwako, na Ututengenezee mwongozo katika jambo letu.

اِذْ اَوَى الْفِتْيَةُ اِلَى الْكَهْفِ فَقَالُوْا رَبَّنَآ اٰتِنَا مِنْ لَّدُنْكَ رَحْمَةً وَّهَيِّئْ لَنَا مِنْ اَمْرِنَا رَشَدًا ﴿١١﴾

12. Hivyo tukawazuia wasisikilize habari za ulimwengu wa nje kwa miaka michache.

فَضَرَبْنَا عَلٰٓى اٰذَانِهِمْ فِي الْكَهْفِ سِنِيْنَ عَدَدًا ﴿١٢﴾

13. Kisha Tukawainua ili Tujulishe ni lipi katika makundi mawili litakalohesabu sawasawa muda waliokaa.

ثُمَّ بَعَثْنٰهُمْ لِنَعْلَمَ اَيُّ الْحِزْبَيْنِ اَحْصٰى لِمَا لَبِثُوْٓا اَمَدًا ﴿١٣﴾ ع ١٣

FUNGU 2

14. Sisi Tunakusimulia habari zao kwa haki: Hakika wao ni vijana waliomwamini Mola wao, nasi Tukawazidishia mwongozo.

نَحْنُ نَقُصُّ عَلَيْكَ نَبَاَهُمْ بِالْحَقِّ ۭ اِنَّهُمْ فِتْيَةٌ اٰمَنُوْا بِرَبِّهِمْ وَزِدْنٰهُمْ هُدًى ﴿١٤﴾

15. Na Tukaiimarisha mioyo yao, waliposimama na wakasema: Mola wetu ni Mola wa mbingu na ardhi, hatutamwita kabisa mungu mwingine badala Yake; (hapo) bila shaka tutakuwa tumesema uovu uliopitiliza.

وَّرَبَطْنَا عَلٰي قُلُوْبِهِمْ اِذْ قَامُوْا فَقَالُوْا رَبُّنَا رَبُّ السَّمٰوٰتِ وَالْاَرْضِ لَنْ نَّدْعُوَا۟ مِنْ دُوْنِهٖٓ اِلٰهًا لَّقَدْ قُلْنَآ اِذًا شَطَطًا ﴿١٥﴾

---

wale wa asili waliokuwa wakimwabudu Mungu Mmoja. Wameitwa *Watu wa Mwandiko* yumkini kwa sababu kila namna ya kitu wanachokitengeneza lazima wakiandike.

Aya 12. *Dharabnaa 'alaa aadhaanihim,* "Tukaziba masikio yao." Neno *dharaba* lina maana nyingi zilizo mbalimbali. Wanasema *Dharaba 'alaa yadihii,* maana yake alimzuia kufanya jambo alilokuwa amekwisha lianza *Dharabnaa 'alaa aadhaanihim,* maana yake ni Tuliwalaza kwa kuwazuilia sauti yo yote isipenye katika masikio yao, na kuwafanya waamke (Lane na Akrab).

Aya hii inaonyesha ya kuwa kwa miaka mingi wale Watu wa Pango hawakuwa wakipata habari za nje.

Aya 14. Aya hii inaonyesha ya kuwa hadithi nyingi za upuuzi zilikuwa zimeenea katika siku za Mtume *s.a.w.* Lakini habari zao za kweli ni hizi ya kuwa walikuwa vijana wenye tabia njema ambao walijitoa kabisa kwa ajili ya Mola wao, na imani yao iliendelea kuzidi walipotiwa taabuni.

Aya 15. Ingawa watu hao waliwataabisha bila kuwaonea huruma, lakini hawakuogopa kushika dini yao. Allah aliimarisha mioyo yao na akawapa imani madhubuti kabisa.

16. Hawa watu wetu wamewashika waungu (wengine) badala Yake. Kwa nini hawaleti juu yao dalili bayana? Basi ni nani mdhalimu mkubwa kuliko yule amtungiaye Allah uwongo?

17. Na mnapokuwa mmejitenga nao na vile wanavyoviabudu badala ya Allah, basi kimbilieni pangoni; Atawafungulieni Mola wenu katika rehema Zake na kuwafanyieni wepesi katika mambo yenu.

18. Na unaliona jua linapopanda linapita mbali na pango lao upande wa kuume, na linapokuchwa linawakata upande wa kushoto, nao wamo katika uwazi ndani yake. Hizo ni katika Ishara za Allah. Ambaye Allah Anamwongoza, basi yeye ndiye aliyeongoka; na Anayemhukumu kupotea, basi hutampatia rafiki wa kumuongoza.

هٰٓؤُلَآءِ قَوْمُنَا اتَّخَذُوْا مِنْ دُوْنِهٖٓ اٰلِهَةً ؕ
لَوْلَا يَاْتُوْنَ عَلَيْهِمْ بِسُلْطٰنٍۢ بَيِّنٍ ؕ فَمَنْ
اَظْلَمُ مِمَّنِ افْتَرٰى عَلَى اللّٰهِ كَذِبًا ﴿١٥﴾
وَاِذِ اعْتَزَلْتُمُوْهُمْ وَمَا يَعْبُدُوْنَ اِلَّا
اللّٰهَ فَاْوٗٓا اِلَى الْكَهْفِ يَنْشُرْ لَكُمْ رَبُّكُمْ
مِّنْ رَّحْمَتِهٖ وَيُهَيِّئْ لَكُمْ مِّنْ اَمْرِكُمْ
مِّرْفَقًا ﴿١٦﴾
وَتَرَى الشَّمْسَ اِذَا طَلَعَتْ تَّزٰوَرُ عَنْ
كَهْفِهِمْ ذَاتَ الْيَمِيْنِ وَاِذَا غَرَبَتْ
تَّقْرِضُهُمْ ذَاتَ الشِّمَالِ وَهُمْ فِيْ فَجْوَةٍ
مِّنْهُ ؕ ذٰلِكَ مِنْ اٰيٰتِ اللّٰهِ ؕ مَنْ يَّهْدِ اللّٰهُ
فَهُوَ الْمُهْتَدِ ۚ وَمَنْ يُّضْلِلْ فَلَنْ تَجِدَ لَهٗ
وَلِيًّا مُّرْشِدًا ﴿١٧﴾ ع ١٤

Aya 16. Watu wa Pango wanaposema, "Hao ndio watu wetu" inaonyesha ya kuwa watu wao walikuwa wanaabudu masanamu, yaani Warumi.

Aya 17. Aya hii inaonyesha ya kwamba watu wa pangoni hawakuwa waliotawanyika ovyo, bali walikuwa na umoja wa dini na mara kwa mara wakikutana faraghani. Inaonekana walipatana ya kwamba wakizidi kutaabishwa wahamie katika pango fulani maalum.

Aya 18. Aya hii inaeleza mahali lilipokuwa lile pango. Inaonekana ya kwamba watu wanaotajwa juu waliishi katika pande za juu sana kaskazini, na pango lilikuwa kwa namna ambayo lilielekea kaskazini-ya-magharibi: maana mahali panapoelekea hivyo ndipo hupitwa na jua toka kulia kwenda kushoto.

Neno *fajwah* (uwazi) linaonyesha ya kuwa pango lile lilikuwa na eneo kubwa . Mapango ya kuzikia watu yaliyoko Rumi yaitwayo *catacombs* yanayoonekana hata leo yanathibitisha jambo hili. Mapango hayo ni mapana sana na yanakadiriwa kuwa na masafa ya maili zaidi ya 870. Pia inaonekana ya kwamba pango hilo liliingiza nuru ndogo kabisa. Pango hilo lilifanywa kwa namna ambayo lifae kuwa mahali pa kujifichia. Jerome Mt. aliyelizuru pango hilo katika karne ya nne ya Kristo anasema, "Lina giza mno hata inaonekana usemi wa Nabii (Zaburi 55:15) umetimia. 'Na washuke kuzimu wangali hai.' Ni kwa nadra tu nuru inaingia kupunguza tisho la giza, na hata hivyo si sana kwa dirisha kama iingiavyo kwa tundu" (Enc. Brit., 11th edition vol. v, p. 491).

FUNGU 3

وَ تَحْسَبُهُمْ اَيْقَاظًا وَّ هُمْ رُقُوْدٌ ۚ وَّنُقَلِّبُهُمْ ذَاتَ الْيَمِيْنِ وَذَاتَ الشِّمَالِ ۖ وَكَلْبُهُمْ بَاسِطٌ ذِرَاعَيْهِ بِالْوَصِيْدِ ؕ لَوِ اطَّلَعْتَ عَلَيْهِمْ لَوَلَّيْتَ مِنْهُمْ فِرَارًا وَّلَمُلِئْتَ مِنْهُمْ رُعْبًا ﴿١٩﴾

19. Na unawadhani wa macho hali wamelala; na Tutawageuza upande wa kulia na upande wa kushoto, na mbwa wao akinyosha mikono yake kizingitini. Kama ungewaona, hakika ungegeuka kuwakimbia, na hakika ungejazwa na hofu juu yao.

وَكَذٰلِكَ بَعَثْنٰهُمْ لِيَتَسَآءَلُوْا بَيْنَهُمْ ؕ قَالَ قَآئِلٌ مِّنْهُمْ كَمْ لَبِثْتُمْ ؕ قَالُوْا لَبِثْنَا يَوْمًا اَوْ بَعْضَ يَوْمٍ ؕ قَالُوْا رَبُّكُمْ اَعْلَمُ بِمَا لَبِثْتُمْ ؕ فَابْعَثُوْۤا اَحَدَكُمْ بِوَرِقِكُمْ هٰذِهٖۤ اِلَى الْمَدِيْنَةِ فَلْيَنْظُرْ اَيُّهَاۤ اَزْكٰى طَعَامًا فَلْيَاْتِكُمْ بِرِزْقٍ مِّنْهُ وَلْيَتَلَطَّفْ وَلَا يُشْعِرَنَّ بِكُمْ اَحَدًا ﴿٢٠﴾

20. Na kadhalika Tuliwainua ili waulizane baina yao. Akasema msemaji katika wao: Mmekaa muda gani? Wakasema: Tumekaa siku moja au sehemu ya siku. (Wengine) wakasema: Mola wenu Anajua zaidi muda mliokaa. Basi mtumeni mmoja wenu pamoja na fedha yenu hii, mjini; na akatazame chakula cha nani ni kizuri zaidi kisha awaleteeni chakula katika hicho. Na apeleleze kwa hila wala asiwatajeni kabisa kwa ye yote.

اِنَّهُمْ اِنْ يَّظْهَرُوْا عَلَيْكُمْ يَرْجُمُوْكُمْ اَوْ يُعِيْدُوْكُمْ فِيْ مِلَّتِهِمْ وَلَنْ تُفْلِحُوْۤا اِذًا اَبَدًا ﴿٢١﴾

21. Maana kama wao wakiwashindeni watawapigeni mawe au kuwarudisheni katika dini yao na ndipo hamtafaulu kamwe.

Kwa kutaja Pango linaloelekea kaskazini, Allah alikusudia kuwahadharisha Waislamu ya kwamba adui yao yuko upande wa kaskazini, ambaye wajihadhari sana naye. Waislamu walipuuza kutahadharishwa huko na wakashindwa kwa urahisi na maadui zao hao. Waislamu, badala ya kuungana pamoja, walipigana wenyewe kwa wenyewe na wakampa adui nafasi. Fitina ya Banu Abbas wa Baghdad na namna chafu ya kutaka kwao msaada wa ufalme wa Byzantine wa Constantinople, na upande mwingine, fitina ya Waarabu wa Spain na serikali ya Pope wa Wakatoliki, ni mambo yaliyowateremsha Waislamu pole pole katika kuangamia.

Aya 19. Sasa hapa zinaelezwa habari za Wakristo waliokuwa siku za Mtume *s.a.w.* ambao walikuwa pande za kaskazini. Waislamu wanaonywa ya kuwa ingawa Wakristo hao wamelala lakini mara wataamka na wataenea dunia na kuitawala.

Maneno haya, *Mbwa wao akinyosha mikono yake kizingitini,* yanaonyesha namna Wakristo wanavyompenda mbwa.

Aya 20. *Tuliwainua,* mradi wake ni kuinuka kwa Wakristo na kupata maendeleo makubwa baadaye.

وَكَذٰلِكَ اَعْثَرْنَا عَلَيْهِمْ لِيَعْلَمُوْٓا اَنَّ
وَعْدَ اللّٰهِ حَقٌّ وَّاَنَّ السَّاعَةَ لَا رَيْبَ فِيْهَا ۚ
اِذْ يَتَنَازَعُوْنَ بَيْنَهُمْ اَمْرَهُمْ فَقَالُوا
ابْنُوْا عَلَيْهِمْ بُنْيَانًا ۗ رَبُّهُمْ اَعْلَمُ بِهِمْ ۗ
قَالَ الَّذِيْنَ غَلَبُوْا عَلٰٓى اَمْرِهِمْ
لَنَتَّخِذَنَّ عَلَيْهِمْ مَّسْجِدًا ﴿٢١﴾

22. Na hivyo Tukawatambulisha kwa watu ili wapate kujua ya kwamba ahadi ya Allah ni kweli, na ya kwamba saa ile haina shaka. (Na kumbukeni) walipozozana baina yao juu ya jambo lao, na wakasema: Jengeni jengo juu yao. Mola wao Anawajua sana. Wakasema wale walioshinda katika shauri lao: Bila shaka sisi tutajenga msikiti juu yao.

سَيَقُوْلُوْنَ ثَلٰثَةٌ رَّابِعُهُمْ كَلْبُهُمْ ۚ
وَيَقُوْلُوْنَ خَمْسَةٌ سَادِسُهُمْ كَلْبُهُمْ
رَجْمًاۢ بِالْغَيْبِ ۚ وَيَقُوْلُوْنَ سَبْعَةٌ
وَّثَامِنُهُمْ كَلْبُهُمْ ۗ قُلْ رَّبِّيْٓ اَعْلَمُ
بِعِدَّتِهِمْ مَّا يَعْلَمُهُمْ اِلَّا قَلِيْلٌ ۗ فَلَا
تُمَارِ فِيْهِمْ اِلَّا مِرَآءً ظَاهِرًا ۖ وَّلَا
تَسْتَفْتِ فِيْهِمْ مِّنْهُمْ اَحَدًا ﴿٢٢﴾ ع ١٥

23. (Wengine) wakasema: Walikuwa watatu, wa nne wao ni mbwa wao; na (wengine) wakasema: Walikuwa watano, wa sita wao ni mbwa wao; kwa kukisia yasiyoonekana. Na (wengine) wakasema: Walikuwa saba na wa nane wao ni mbwa wao. Sema: Mola wangu Ndiye Ajuaye sawasawa idadi yao ya kweli ilikuwa kiasi gani. Ni wachache sana wanaojua habari za watu hao. Basi usibishane juu yao ila kwa mabishano yanayoshinda, wala usiulize habari zao kwa yeyote.

FUNGU 4

وَلَا تَقُوْلَنَّ لِشَايْءٍ اِنِّيْ فَاعِلٌ ذٰلِكَ
غَدًا ﴿٢٣﴾

24. Wala usiseme kamwe juu ya jambo: Hakika mimi lazima nitalifanya kesho.

Aya 22. *Jengeni jengo juu yao.* Ina maana ya kujenga mnara wa kumbukumbu mahali yalipo makaburi yao. Hapa Qur'an inarejea tena habari za Wakristo wa zamani wa pangoni na kuonyesha alama yao moja maarufu ya kuwa mataifa ya Wakristo watajenga makanisa kwa ukumbusho wa watakatifu wao waliokufa. Mayahudi na Waislamu hawajengi masinagogi na misikiti kwa kuwakumbuka mawalii wao. Wakristo tu ndio wafanyao hivi, na hata wanawazika wafu wao ndani ya viwanja vya makanisa.

Aya 23. *Mola wangu ndiye Ajuaye sawasawa hesabu yao.* Maneno haya yanaonyesha ya kwamba watu walibishana bure juu ya hesabu hasa ya watu wa pangoni, maana Allah tu ndiye

25. Isipokuwa Allah Apende. Na umkumbuke Mola wako unaposahau, na sema: Asaa Mola wangu Ataniongoza njia iliyo karibu zaidi na mwongozo kuliko hii.

26. Na walikaa katika pango lao miaka mia tatu na wakazidisha (miaka) tisa.

27. Sema: Allah Anaujua barabbara muda waliokaa. Ni Zake siri za mbingu na ardhi. Ndiye Aonaye sana na Asikiaye sana! Wao hawana mlinzi badala Yake, wala Yeye Hamshirikishi ye yote katika hukumu Yake.

28. Na usome yaliyofunuliwa kwako katika Kitabu cha Mola wako; hakuna awezaye kubadilisha maneno Yake; nawe hutapata kimbilio kinyume Chake.

29. Na ujiweke pamoja na wale wanaomwomba Mola wao asubuhi na jioni wakitaka radhi Yake, wala macho yako yasiwaruke, kwa kutaka mapambo ya maisha ya dunia; wala usimtii ambaye Tumeughafilisha moyo wake kwa kutukumbuka, naye akafuata matamanio yake, na mambo yake yamepita kiasi.

إِلَّآ أَن يَشَآءَ ٱللَّهُ ۚ وَٱذْكُر رَّبَّكَ إِذَا
نَسِيتَ وَقُلْ عَسَىٰٓ أَن يَهْدِيَنِ رَبِّى
لِأَقْرَبَ مِنْ هَٰذَا رَشَدًا ﴿٢٤﴾
وَلَبِثُوا۟ فِى كَهْفِهِمْ ثَلَٰثَ مِا۟ئَةٍ سِنِينَ
وَٱزْدَادُوا۟ تِسْعًا ﴿٢٥﴾
قُلِ ٱللَّهُ أَعْلَمُ بِمَا لَبِثُوا۟ ۖ لَهُۥ غَيْبُ
ٱلسَّمَٰوَٰتِ وَٱلْأَرْضِ ۖ أَبْصِرْ بِهِۦ وَأَسْمِعْ ۚ
مَا لَهُم مِّن دُونِهِۦ مِن وَلِىٍّ ۖ وَلَا يُشْرِكُ
فِى حُكْمِهِۦٓ أَحَدًا ﴿٢٦﴾
وَٱتْلُ مَآ أُوحِىَ إِلَيْكَ مِن كِتَابِ رَبِّكَ ۖ
لَا مُبَدِّلَ لِكَلِمَٰتِهِۦ ۚ وَلَن تَجِدَ مِن دُونِهِۦ
مُلْتَحَدًا ﴿٢٧﴾
وَٱصْبِرْ نَفْسَكَ مَعَ ٱلَّذِينَ يَدْعُونَ
رَبَّهُم بِٱلْغَدَوٰةِ وَٱلْعَشِىِّ يُرِيدُونَ
وَجْهَهُۥ ۖ وَلَا تَعْدُ عَيْنَاكَ عَنْهُمْ ۚ تُرِيدُ
زِينَةَ ٱلْحَيَوٰةِ ٱلدُّنْيَا ۖ وَلَا تُطِعْ مَنْ
أَغْفَلْنَا قَلْبَهُۥ عَن ذِكْرِنَا وَٱتَّبَعَ هَوَىٰهُ
وَكَانَ أَمْرُهُۥ فُرُطًا ﴿٢٨﴾

Aya 26. Aya hii inaonyesha, Wakristo waliendelea kusumbuliwa kwa miaka 309 mfululizo na kila mara wanakimbilia pangoni ili kujificha. Muda wa kutaabishwa kwa Wakristo ulianza wakati wa kusulubiwa Yesu mwaka wa 28 A.D. na ukaisha wakati mfalme Constatine alipoingia katika dini ya Kikristo mwaka 337 A.D. (Enc. Brit. 14th edition, vol. V), yaani miaka 309 kama inavyosema Qur'an.

Aya 28. Aya hii inaonyesha wazi ya kuwa maelezo ya juu kwa habari za Watu wa Pango, hayaelezwi kwa jiha ya kisa cha kupendeza, bali yanaeleza matukio ya zamani ya mambo makubwa ya dini, na papo yanawahadharisha Waislamu wawe tayari kukutana na taabu kama walizopata Watu wa Pango. Kwa hakika kama asemavyo Ibni Abbas, Mtume *s.a.w.* alisema ya kwamba *As'haabul-kahf* (Watu wa pango) ni wafuasi wa Imam Mahdi (Manthur).

Aya 29. Aya hii inazidi kuhakikisha ya kwamba Aya zilizotangulia zina bishara za maana sana. Kwa hakika hapa tunaambiwa ya kwamba wakati wa kustawi na kupata nguvu mataifa ya

وَقُلِ الْحَقُّ مِنْ رَّبِّكُمْ ۟ فَمَنْ شَآءَ
فَلْيُؤْمِنْ وَّمَنْ شَآءَ فَلْيَكْفُرْ ۙ اِنَّآ
اَعْتَدْنَا لِلظّٰلِمِيْنَ نَارًا ۙ اَحَاطَ بِهِمْ
سُرَادِقُهَا ؕ وَاِنْ يَّسْتَغِيْثُوْا يُغَاثُوْا بِمَآءٍ
كَالْمُهْلِ يَشْوِى الْوُجُوْهَ ؕ بِئْسَ
الشَّرَابُ ؕ وَسَآءَتْ مُرْتَفَقًا ۝٢٩

30. Na sema: Ukweli umetoka kwa Mola wenu, basi anayependa akubali, na anayependa basi akatae. Hakika Tumewaandalia wadhalimu Moto ambao uwa wake utawazunguka. Na wakiomba msaada, watasaidiwa kwa maji kama shaba iliyoyeyuka, yatakayo-ziunguza nyuso. Kinywaji kibaya kilioje, na mahali pabaya palioje pa kupumzikia!

اِنَّ الَّذِيْنَ اٰمَنُوْا وَعَمِلُوا الصّٰلِحٰتِ اِنَّا
لَا نُضِيْعُ اَجْرَ مَنْ اَحْسَنَ عَمَلًا ۝٣٠

31. Hakika wale walioamini na kufanya vitendo vizuri - hakika sisi Hatupotezi ujira wa yule anayefanya vitendo vizuri.

اُولٰٓئِكَ لَهُمْ جَنّٰتُ عَدْنٍ تَجْرِىْ مِنْ
تَحْتِهِمُ الْاَنْهٰرُ يُحَلَّوْنَ فِيْهَا مِنْ اَسَاوِرَ
مِنْ ذَهَبٍ وَّيَلْبَسُوْنَ ثِيَابًا خُضْرًا مِّنْ
سُنْدُسٍ وَّاِسْتَبْرَقٍ مُّتَّكِـِٕيْنَ فِيْهَا عَلَى
الْاَرَآئِكِ ؕ نِعْمَ الثَّوَابُ ؕ وَحَسُنَتْ
مُرْتَفَقًا ۝٣١

32. Hao watapata Bustani za milele, itapita mito chini yao. Humo watapambwa bangili za dhahabu na watavaa nguo za kijani za hariri laini, na hariri nzito, humo wakiegemea matakia juu ya vitanda vilivyopambwa. Ni malipo mazuri yaliyoje, na mahali bora palioje pa kupumzikia.

ع ١٦

FUNGU 5

وَاضْرِبْ لَهُمْ مَّثَلًا رَّجُلَيْنِ جَعَلْنَا
لِاَحَدِهِمَا جَنَّتَيْنِ مِنْ اَعْنَابٍ
وَّحَفَفْنٰهُمَا بِنَخْلٍ وَّجَعَلْنَا بَيْنَهُمَا
زَرْعًا ۝٣٢

33. Na uwapigie mfano wa watu wawili: mmoja wao Tulimfanyia bustani mbili za mizabibu, na Tukazizungushia mitende, na pia kati ya hizo mbili Tukatia shamba la nafaka.

Wakristo, duniani watakuwako watu ambao ni Waislamu wa kweli watakaoshughulika usiku na mchana kumwabudu Allah. Wakati huo wa Imam Mahdi, kutakuwa na Waislamu-jina ambao tumaini lao la kutukuka Uislamu litakuwa katika vifaa vya dunia, nao watawadharau wafuasi maskini, wasio na jina, wa Imam Mahdi kwa kukazana kwao na ibada. Aya hii inawaonya Waislamu ya kwamba kufanikiwa kwa Uislamu kutategemea kuomba dua na kumwabudu Allah.

Zaidi ya hayo Aya hii inaonyesha mambo matatu ambayo ni sababu kubwa za misiba na taabu zitakazowafikia Waislamu wakati huo: (a) wataacha kusali na kumwabudu Mungu, (b) kuipenda dunia kutakuwa ndiyo shauku yao kubwa; na (c) watazama kabisa katika kutafuta starehe na anasa. Lakini kupona kwao kutakuwa katika kubadilisha kwao mawazo na mipango yao kabisa.

Aya 33. Aya hii kwa sura ya mfano inaanza kueleza hali za Waislamu na Wakristo katika

كِلْتَا الْجَنَّتَيْنِ اٰتَتْ اُكُلَهَا وَلَمْ تَظْلِمْ مِّنْهُ شَيْـًٔا ۙ وَّفَجَّرْنَا خِلٰلَهُمَا نَهَرًا ﴿٣٤﴾

34. Hizi bustani mbili zilizaa matunda yao wala hazikupunguza cho chote; na ndani yake Tukatiririsha mto.

وَّكَانَ لَهٗ ثَمَرٌ ۚ فَقَالَ لِصَاحِبِهٖ وَهُوَ يُحَاوِرُهٗٓ اَنَا اَكْثَرُ مِنْكَ مَالًا وَّاَعَزُّ نَفَرًا ﴿٣٥﴾

35. Naye alikuwa na matunda (mengi), basi akamwambia mwenzake hali akibishana naye, mimi nina mali nyingi kuliko wewe na (nina) nguvu zaidi kwa wafuasi.

وَدَخَلَ جَنَّتَهٗ وَهُوَ ظَالِمٌ لِّنَفْسِهٖ ۚ قَالَ مَآ اَظُنُّ اَنْ تَبِيْدَ هٰذِهٖٓ اَبَدًا ﴿٣٦﴾

36. Na akaingia bustani yake hali ya kujidhulumu nafsi yake. Akasema: Sidhani abadan kuwa hii itaharibika.

وَّمَآ اَظُنُّ السَّاعَةَ قَآئِمَةً ۙ وَّلَئِنْ رُّدِدْتُّ اِلٰى رَبِّيْ لَاَجِدَنَّ خَيْرًا مِّنْهَا مُنْقَلَبًا ﴿٣٧﴾

37. Wala sidhani kuwa saa (ile) itatokea. Na kama nikirudishwa kwa Mola wangu, bila shaka nitakuta kikao chema kuliko hiki.

---

siku za baadaye.

Namna na mpango wa maneno ya mazungumzo haya unaonyesha waziwazi ya kuwa si mazungumzo hasa baina ya watu wawili, bali ni sura inayoonyesha kwa namna ya hadithi ya hali ya mataifa mawili ya wakati fulani. Mazungumzo hayo yanaonyesha kudhalilika na kupooza kwa Waislamu na nguvu na ustawi wa mataifa ya Kikristo ya pande za Magharibi za dunia katika siku za baadaye - yaani hizi siku zetu.

Sasa methali ni kama ndoto hutaka kufasiriwa, na Aya hii na zifuatazo kadha wa kadha ziko katika maneno ya fumbo na haiwezekani kuona uzuri wao kamili bila kuziwekea mpango ambao hivi zilivyo unaonekana haupo. Katika lugha ya ndoto "bustani" mradi wake ni mke, watoto, utajiri na maisha yaliyojaa raha; pengine huwa na mradi wa kambi ya askari na Makao Makuu ya jeshi la vita. "Zabibu mradi wake ni vyakula vingi vinavyoweza kuwekwa akiba na kukaa kwa muda mrefu; "mitende" mradi wake ni kuwa na mamlaka juu ya kundi kubwa la watu; "nafaka" kwa mfalme huwa na mradi wa kuupanua ufalme wake, na kwa watu wengine huwa na mradi wa "kazi" zao. "Mto" mradi wake ni mtu mkubwa, na "matunda" maana yake ni njia mpya za kupatia heshima (Ta'tiir-ul-Anaam).

Mfano huu unaeleza hali ya watu wawili. Mmoja alikuwa na bustani mbili, kwa tafsiri ya kwamba Allah alimpa mali mengi na watoto katika nyakati mbili mbalimbali za maisha yake. Tafsiri hii inatiwa nguvu na Aya 35 hapa chini, mtu huyo anaposema: *Nina mali nyingi kuliko wewe na (nina) nguvu zaidi kwa wafuasi.*

Maneno haya, *Tukazizungushia mitende*, yanaonyesha ya kwamba mtu huyo atalinda mali zake na watoto wake na dola zake kwa nguvu ya majeshi ya vita.

Na maneno haya, *Kati ya hizo mbili Tukatia shamba la nafaka.* Yanaonyesha ya kwamba katikati ya bustani mbili kutakuwa na mali za kawaida tu ambazo hazitalindwa kwa nguvu sana.

Aya 35. Maana ya mfano huu wote ni hii. Mwanzo wa sura hii ilielezwa ya kuwa Mtume *s.a.w.* alikuwa amekwisha fikisha ujumbe wa Mungu kwa watu wa Makka, na sasa atawafikishia ujumbe Wakristo ambao husema kuwa Mungu amepanga mwana. Tena zikatajwa habari za Wakristo wa zamani waliovumilia mateso yasiyokadirika kwa ajili ya kuamini Umoja wa Mwenyezi

قَالَ لَهٗ صَاحِبُهٗ وَهُوَ يُحَاوِرُهٗٓ اَكَفَرْتَ بِالَّذِيْ خَلَقَكَ مِنْ تُرَابٍ ثُمَّ مِنْ نُّطْفَةٍ ثُمَّ سَوّٰىكَ رَجُلًا ﴿٣٨﴾

38. Mwenzake akamwambia, hali akibishana naye: Je unamkufuru Yule Aliyekuumba kutoka katika vumbi, tena kwa tone la manii, kisha Akakufanya mtu kamili?

لٰكِنَّا۠ هُوَ اللّٰهُ رَبِّيْ وَلَآ اُشْرِكُ بِرَبِّيْٓ اَحَدًا ﴿٣٩﴾

39. Lakini (mimi naamini) Yeye Allah Ndiye Mola wangu, wala simshirikishi Mola wangu na ye yote.

وَلَوْلَآ اِذْ دَخَلْتَ جَنَّتَكَ قُلْتَ مَا شَآءَ اللّٰهُ ۙ لَا قُوَّةَ اِلَّا بِاللّٰهِ ۚ اِنْ تَرَنِ اَنَا اَقَلَّ مِنْكَ مَالًا وَّوَلَدًا ﴿٣٩﴾

40. Na ulipoingia katika bustani yako mbona hukusema: Apendayo Allah (ndiyo huwa), nguvu haipatikani ila kwa Allah. Kama unaniona mimi ninayo mali kidogo na watoto wachache kuliko wewe.

فَعَسٰى رَبِّيْٓ اَنْ يُّؤْتِيَنِ خَيْرًا مِّنْ جَنَّتِكَ وَيُرْسِلَ عَلَيْهَا حُسْبَانًا مِّنَ السَّمَآءِ فَتُصْبِحَ صَعِيْدًا زَلَقًا ﴿٤٠﴾

41. Basi huenda Mola wangu Akanipa kilicho bora kuliko bustani yako, na kuipelekea mapigo ya radi kutoka mbinguni na ikawa ardhi tupu inayoteleza;

اَوْ يُصْبِحَ مَآؤُهَا غَوْرًا فَلَنْ تَسْتَطِيْعَ لَهٗ طَلَبًا ﴿٤١﴾

42. Au maji yake yazame chini sana kisha hautakuwa na uwezo asilan wa kuyarejesha.

Mungu, na wenzao waliokuja baada yao wakawa waabuduo masanamu, na wakazama kabisa katika kutafuta mali za dunia.

Mfano huu wa Qur'an unafanana na mfano wa shamba la mizabibu uliomo katika Injili (Marko 12:1-2; Matt. 21:33-46 na Luka 20:9-19). Mfano huo unaeleza habari za mataifa mawili - Waislamu na Wakristo. Katika mfano wa Qur'an, Bwana wa Shamba ni Wakristo, na "mizabibu" ni kuzidi kwa mali zao na watoto. Uwa wa mitende unaonyesha majeshi yao ya vita ambayo katika siku zao za nguvu na utukufu yatalinda mali zao.

Maneno haya, *Nina mali nyingi kuliko wewe na (nina) nguvu zaidi kwa wafuasi,* yana maana ya kwamba mataifa ya Wakristo yafanya utajiri wao na nguvu ya utawala wao kuwa hoja ya ukweli wa dini yao, wakilinganisha na umaskini na kuwa nyuma kwa Waislamu.

Aya 41. Maneno haya, *Kuipelekea mapigo ya radi kutoka mbinguni,* yanaonyesha kuwa hakutakuwa nguvu hapa duniani itakayoweza kuishinda nguvu ya vita ya mataifa ya Kikristo. Mungu Mwenyewe ndiye atatengeneza njia zitakazowapeleka kwenye maangamizo. Ni hii nguvu isiyoshindika ya *Yaajuuj* na *Maajuuj* (Gog na Magog) iliyotajwa na Mtume *s.a.w.* aliposema "Hakuna atakayekuwa na nguvu ya kupigana nao" (Muslim, sura ya *Dajaal*).

وَاُحِيْطَ بِثَمَرِهٖ فَاَصْبَحَ يُقَلِّبُ كَفَّيْهِ
عَلٰى مَآ اَنْفَقَ فِيْهَا وَهِيَ خَاوِيَةٌ عَلٰى
عُرُوْشِهَا وَيَقُوْلُ يٰلَيْتَنِيْ لَمْ اُشْرِكْ
بِرَبِّيْٓ اَحَدًا ﴿٤٣﴾

43. Na matunda yake yakaangamizwa na akawa kutukusa viganja vyake kwa ajili ya yale aliyoigharamia (bustani), nayo imeanguka juu ya mapaa yake, na akasema: Laiti nisingalimshirikisha Mola wangu na ye yote!

وَلَمْ تَكُنْ لَّهٗ فِئَةٌ يَّنْصُرُوْنَهٗ مِنْ دُوْنِ اللّٰهِ
وَمَا كَانَ مُنْتَصِرًا ﴿٤٤﴾

44. Wala hakuwa na kundi la kumsaidia kinyume na Allah, wala mwenyewe hakuweza kujisaidia.

هُنَالِكَ الْوَلَايَةُ لِلّٰهِ الْحَقِّ ۭ هُوَ خَيْرٌ ثَوَابًا
وَّخَيْرٌ عُقْبًا ﴿٤٤﴾ ع ۝١٧

45. Katika nyakati kama hizo mamlaka yote yanakuwa ni ya Allah tu, Aliye Mkweli. Yeye ni Mbora kwa kuleta malipo na ni Mbora kwa kuleta matokeo mema.

FUNGU 6

وَاضْرِبْ لَهُمْ مَّثَلَ الْحَيٰوةِ الدُّنْيَا كَمَاۗءٍ
اَنْزَلْنٰهُ مِنَ السَّمَاۗءِ فَاخْتَلَطَ بِهٖ نَبَاتُ
الْاَرْضِ فَاَصْبَحَ هَشِيْمًا تَذْرُوْهُ
الرِّيٰحُ ۭ وَكَانَ اللّٰهُ عَلٰي كُلِّ شَيْءٍ
مُّقْتَدِرًا ﴿٤٥﴾

46. Na uwapigie mfano wa maisha ya dunia: ni kama maji Tuyateremshayo kutoka mawinguni, kisha huchanganyika nayo mimea ya ardhi, kisha ikawa majani makavu yaliyovunjika vunjika ambayo upepo huyasambaza. Na Allah Ana uwezo juu ya kila kitu.

اَلْمَالُ وَالْبَنُوْنَ زِيْنَةُ الْحَيٰوةِ الدُّنْيَا ۚ
وَالْبٰقِيٰتُ الصّٰلِحٰتُ خَيْرٌ عِنْدَ رَبِّكَ
ثَوَابًا وَّخَيْرٌ اَمَلًا ﴿٤٦﴾

47. Mali na watoto ni mapambo ya maisha ya dunia. Na vitendo vizuri vibakiavyo ndiyo bora mbele ya Mola wako kwa malipo na tumaini bora.

Aya 43. *Khaawiyatun 'alaa 'uruushihaa,* "Imeanguka juu ya mapaa yake." Mradi wa bustani ni miji ya fahari yenye majumba marefu ya Wakristo. Aya hii inaonyesha ya kwamba misiba itawafikia Wakristo mfululizo, na miji yao iliyostawi na kutajirika itabomoka hadi chini, na kutubu kwao kwa wakati huo hakutafaa kitu.

Aya 45. Aya hii inakumbusha kwa mkazo ukweli wa daima ya kuwa mamlaka yote ni ya Allah, na ya kwamba adhabu Yake inapowafikia watu hakuna wa kuwaokoa. Pia inaonyesha ya kuwa Aya hizi chache zilizotangulia zinabashiria kuangamia mataifa ya Wakristo.

وَيَوْمَ نُسَيِّرُ الْجِبَالَ وَتَرَى الْاَرْضَ بَارِزَةً ۙ وَّحَشَرْنٰهُمْ فَلَمْ نُغَادِرْ مِنْهُمْ اَحَدًا ﴿٤٧﴾

48. Na siku Tutakayoipitisha milima, na utaona (watu wa) ardhi wakienda (vitani), nasi Tutawakusanya wala Hatutamwacha (hata) mmoja katika wao.

وَعُرِضُوْا عَلٰى رَبِّكَ صَفًّا ؕ لَقَدْ جِئْتُمُوْنَا كَمَا خَلَقْنٰكُمْ اَوَّلَ مَرَّةٍ ۭ بَلْ زَعَمْتُمْ اَلَّنْ نَّجْعَلَ لَكُمْ مَّوْعِدًا ﴿٤٨﴾

49. Na watahudhurishwa mbele ya Mola wako safu-safu (na wataambiwa): Bila shaka mmetufikia kama Tulivyowaumbeni mara ya kwanza. Lakini mlidhani ya kuwa Hatukuwawekeeni miadi.

وَوُضِعَ الْكِتٰبُ فَتَرَى الْمُجْرِمِيْنَ مُشْفِقِيْنَ مِمَّا فِيْهِ وَيَقُوْلُوْنَ يٰوَيْلَتَنَا مَالِ هٰذَا الْكِتٰبِ لَا يُغَادِرُ صَغِيْرَةً وَّلَا كَبِيْرَةً اِلَّآ اَحْصٰىهَا ۚ وَوَجَدُوْا مَا عَمِلُوْا حَاضِرًا ؕ وَلَا يَظْلِمُ رَبُّكَ اَحَدًا ﴿٤٩﴾ ع ١٨

50. Na daftari itawekwa (mbele yao); ndipo utawaona wakosefu wanaogopa kwa sababu ya yale yaliyomo; na watasema: Ole wetu! namna gani daftari hii! haiachi dogo wala kubwa ila inalihesabu. Na watakuta waliyoyafanya yamehudhuria; na Mola wako Hamdhulumu ye yote.

FUNGU 7

وَاِذْ قُلْنَا لِلْمَلٰٓئِكَةِ اسْجُدُوْا لِاٰدَمَ فَسَجَدُوْٓا اِلَّآ اِبْلِيْسَ ؕ كَانَ مِنَ الْجِنِّ فَفَسَقَ عَنْ اَمْرِ رَبِّهٖ ؕ اَفَتَتَّخِذُوْنَهٗ وَذُرِّيَّتَهٗٓ اَوْلِيَآءَ مِنْ دُوْنِيْ وَهُمْ لَكُمْ عَدُوٌّ ؕ بِئْسَ لِلظّٰلِمِيْنَ بَدَلًا ﴿٥٠﴾

51. Na (kumbukeni) Tulipowaambia Malaika, Mtiini Adamu, basi wakamtii isipokuwa Ibilisi; alikuwa miongoni mwa majinni, na akavunja amri ya Mola wake. Je mnamshika yeye na wazao wake kuwa marafiki badala Yangu hali ya kwamba hao ni maadui zenu? Ni baya lilioje kwa wadhalimu badilisho hili.

مَآ اَشْهَدْتُّهُمْ خَلْقَ السَّمٰوٰتِ وَالْاَرْضِ وَلَا خَلْقَ اَنْفُسِهِمْ ۖ وَمَا كُنْتُ مُتَّخِذَ الْمُضِلِّيْنَ عَضُدًا ﴿٥١﴾

52. Sikuwashuhudisha kuumbwa kwa mbingu na ardhi wala kuumbwa kwa nafsi zao; wala Sikuwatwaa wapotezao kuwa wasaidizi.

Aya 50. *Na Mola wako Hamdhulumu ye yote.* Maneno haya yanaonyesha ya kuwa adhabu itakuwa kali kabisa, na mwisho wake utakuwa wa taabu sana, lakini yote haya ni matokeo ya matendo yao maovu. Mungu Mwenye huruma hamdhulumu ye yote.

وَيَوْمَ يَقُوْلُ نَادُوْا شُرَكَآءِيَ الَّذِيْنَ زَعَمْتُمْ فَدَعَوْهُمْ فَلَمْ يَسْتَجِيْبُوْا لَهُمْ وَجَعَلْنَا بَيْنَهُمْ مَّوْبِقًا ﴿٥٣﴾

53. Na (kumbukeni) siku Atakayosema: Waiteni washirika Wangu ambao mliwadhani. Basi watawaita, lakini hawatawaitikia; na kati yao Tutatia kinga.

وَرَاَ الْمُجْرِمُوْنَ النَّارَ فَظَنُّوْٓا اَنَّهُمْ مُّوَاقِعُوْهَا وَلَمْ يَجِدُوْا عَنْهَا مَصْرِفًا ﴿٥٤﴾ ع ١٩

54. Na wakosefu watauona Moto, na watajua ya kwamba karibu wao kuangukia humo; wala hawatapata pa kuuepukia.

FUNGU 8

وَلَقَدْ صَرَّفْنَا فِيْ هٰذَا الْقُرْاٰنِ لِلنَّاسِ مِنْ كُلِّ مَثَلٍ ؕ وَكَانَ الْاِنْسَانُ اَكْثَرَ شَيْءٍ جَدَلًا ﴿٥٥﴾

55. Na bila shaka Tumewaelezea watu namna kwa namna katika Qur'an hii kila mfano; lakini mwanadamu amezidi kila kitu kwa ubishi.

وَمَا مَنَعَ النَّاسَ اَنْ يُّؤْمِنُوْٓا اِذْ جَآءَهُمُ الْهُدٰى وَيَسْتَغْفِرُوْا رَبَّهُمْ اِلَّآ اَنْ تَاْتِيَهُمْ سُنَّةُ الْاَوَّلِيْنَ اَوْ يَاْتِيَهُمُ الْعَذَابُ قُبُلًا ﴿٥٦﴾

56. Na hakuna kitu kilichowazuia watu wasiamini na kuomba msamaha kutoka kwa Mola wao mwongozo ulipowafikia, isipokuwa kwamba walichagua kufuata njia ya watu wa zamani pamoja na yale yale yaliyowasibu, au waliisubiri adhabu ya Allah iwakumbe ana kwa ana.

وَمَا نُرْسِلُ الْمُرْسَلِيْنَ اِلَّا مُبَشِّرِيْنَ وَمُنْذِرِيْنَ ۚ وَيُجَادِلُ الَّذِيْنَ كَفَرُوْا بِالْبَاطِلِ لِيُدْحِضُوْا بِهِ الْحَقَّ وَاتَّخَذُوْٓا اٰيٰتِيْ وَمَآ اُنْذِرُوْا هُزُوًا ﴿٥٧﴾

57. Na Hatuwatumi Mitume ila wawe watoaji wa habari njema na waonyaji. Na wale waliokufuru wanajadili kwa uwongo ili kwayo waibatilishe haki; na wakazifanya Aya Zangu na yale waliyoonywa kuwa mzaha.

Aya 54. Neno *Naar,* "Moto," mradi wake ni vita (sura 5:65), na Aya hii inaonyesha ya kuwa mataifa ya pande za Magharibi yataona vita iangamizayo kabisa inawasogelea. Watajaribu wawezavyo kuizuia lakini juhudi yao yote ya kuizuia itakufa bure. Magharibi (Ulaya na Amerika) imekwisha pita ndani ya kiwaka cha vita mbili ziangamizazo kabisa ambazo zimevunja kabisa nguvu yao na sifa yao ulimwenguni, na ustaarabu wao umetiwa msukosuko wa kitisho. Sasa vita ya tatu ya dunia nzima inawakodolea macho!

Aya 57. Aya hii ina maana ya kwamba Ishara huonyeshwa wasioamini ili ziwafae, na wajiponye na adhabu kwa kukubali haki. Lakini wao huwacheka Mitume na kuwaona kama watu

58. Na ni nani mdhalimu mkubwa kuliko yule anayekumbushwa Aya za Mola wake lakini anazipuuza, na akayasahau iliyoyatanguliza mikono yake? Hakika Sisi Tumetia mioyoni mwao vifuniko wasije kuifahamu, na katika masikio yao (Tumetia) uzito. Na ukiwaita kwenye mwongozo ndipo hawatakubali abadan kuongoka.

وَمَنْ اَظْلَمُ مِمَّنْ ذُكِّرَ بِاٰيٰتِ رَبِّهٖ
فَاَعْرَضَ عَنْهَا وَنَسِيَ مَا قَدَّمَتْ يَدٰهُ ؕ اِنَّا
جَعَلْنَا عَلٰى قُلُوْبِهِمْ اَكِنَّةً اَنْ يَّفْقَهُوْهُ
وَفِيْٓ اٰذَانِهِمْ وَقْرًا ؕ وَاِنْ تَدْعُهُمْ اِلَى
الْهُدٰى فَلَنْ يَّهْتَدُوْٓا اِذًا اَبَدًا ۝٥٨

59. Na Mola wako ndiye Msamehevu, Mwenye rehema. Kama Angewakamata kwa sababu ya yale waliyoyachuma, bila shaka Angewahimizia adhabu; lakini wanayo miadi ambayo hawatapata kimbilio kuepukana nayo.

وَرَبُّكَ الْغَفُوْرُ ذُو الرَّحْمَةِ ؕ لَوْ
يُؤَاخِذُهُمْ بِمَا كَسَبُوْا لَعَجَّلَ لَهُمُ
الْعَذَابَ ؕ بَلْ لَّهُمْ مَّوْعِدٌ لَّنْ يَّجِدُوْا
مِنْ دُوْنِهٖ مَوْئِلًا ۝٥٩

60. Na miji hiyo - Tuliwaangamiza walipodhulumu, na Tukawawekea miadi ya maangamizo yao.

وَتِلْكَ الْقُرٰٓى اَهْلَكْنٰهُمْ لَمَّا ظَلَمُوْا
وَجَعَلْنَا لِمَهْلِكِهِمْ مَّوْعِدًا ۝٦٠ ع

FUNGU 9

61. Na (kumbukeni) Musa alipomwambia kijana wake: Sitasimama mpaka nifike penye maungano ya bahari mbili, au niendelee karne na karne.

وَاِذْ قَالَ مُوْسٰى لِفَتٰىهُ لَآ اَبْرَحُ حَتّٰٓى
اَبْلُغَ مَجْمَعَ الْبَحْرَيْنِ اَوْ اَمْضِيَ حُقُبًا ۝٦١

---

wajinga, wapuuzi, wenye akili za kishirikina, na kuwakataa kwa dharau. Lakini wanakubali fikira zilizo nusu-nusu za wana-falsafa wao kana kwamba ni neno la Mungu. Aya hii inaeleza zilivyo fikira za mataifa ya Ulaya juu ya mambo ya dini.

Aya 61. Aya hii inaanza na habari yenye maana sana ya *Israa* (Safari ya njozi ya Usiku) ya Nabii Musa. Kama ilivyoelezwa juu, wafuasi wa Yesu Kristo wamepata nguvu kubwa ya kidunia na ustawi mara mbili katika dunia. Mafanikio haya mawili ya mataifa ya Wakristo yamefananishwa na "bustani mbili" katika Aya 33. Mafanikio yao ya kwanza yalianza na kuingia Ukristo kwa Mfalme wa Kirumi aitwaye Constantine, ambapo Ukristo ukawa dini ya Serikali, na ukaendelea mpaka kuzaliwa Mtume Muhammad *s.a.w.* Na mafanikio yao ya pili na yenye maana zaidi ni ya wakati huu ambao mataifa ya Wakristo ya Ulaya na Amerika yamepata nguvu na heshima kubwa sana, hata mataifa ya Asia na Afrika yamelazimika kuwa chini ya miguu yao. Baina ya hizi "bustani" mbili ulitiririka "mto" (Aya 34). Kama ilivyokwisha elezwa, "bustani mbili" ni bishara ya nyakati mbili za ustawi na mafanikio ya Wakristo. "Mto" unaashiria kuondokea na kupata nguvu Mtume Muhammad s.a.w. Yeye na wafuasi wake wametia athari yao katika historia ya wanadamu katika majira yaliyo katikati ya nyakati mbili za mafanikio ya Wakristo ya zamani na ya sasa.

Sasa, ili kuipa habari hii nzima umbo la habari kamili za historia na kuifanya ionekane nzima iliyounganika, habari ya *Israa* ya Nabii Musa inaelezwa katika Aya hii na zifuatazo. Nabii Musa alitabiri kufika kwa Nabii aliye kama yeye (tazama Kumbukumbu la Torati 18:18 na sura 7:158). Bishara hii imetajwa katika Qur'an sura 73:16. Kwa kutia habari ya *Israa* ya Nabii Musa katikati ya habari za watu wa Pango na za Dhul Qarnain - ambazo ni majira mbili zinazoonyesha maendeleo na mafanikio ya Wakristo - Qur'an imeonyesha ya kwamba yule Nabii aliyebashiriwa kufika katika bishara ya Nabii Musa, ambaye atakuwa kama Musa mwenyewe, alikuwa wa kudhihiri katikati ya nyakati hizi mbili. Hivyo matukio haya yametajwa katika mpango wao wa historia.

Hadithi za upuuzi sana zimeenea juu ya namna na kusudi la Israa ya Nabii Musa. Wafasiri wa Qur'an wanahitilafiana juu ya "Mtumishi wa Mungu" aliyekuwa anatafutwa na Nabii Musa ambaye anatajwa katika Aya ya 66, juu ya jina lake na cheo chake; na kadhalika wanahitilafiana juu ya "kijana" aliyefuatana na Nabii Musa katika "safari" hiyo. Waliposhindwa kufahamu upande wa kiroho wa jambo hili, wengi wao wakaingilia kudhani na kubahatisha, na wamekosea vibaya kabisa.

Hakika ni hii ya kwamba katika Aya 2 ya sura ya 17 *Israa* au kama inavyofasiriwa kuwa Hijra ya Mtume *s.a.w* kuhamia Madina, imetajwa. Pia ikaonyeshwa ni matokeo gani makubwa yatakayotokana na kuhama kule kwa Mtume *s.a.w.* na mafanikio makubwa watakayopata Waislamu. Kadhalika walitahadharishwa na hatari kubwa zilizowangojea, na pia uadui wa Mayahudi na Wakristo. *Israa* ya Nabii Musa imetajwa ili tu kutia mkazo bishara za mafanikio ya Waislamu ya baadaye ambayo yalibashiriwa katika *Israa* ya Mtume Muhammad *s.a.w.;* na pia kubainisha kabisa ya kuwa nguvu na mafanikio ya ajabu ya Wakristo ni kitu cha kupita tu, na baadaye Uislamu utashinda.

Majma'ul Bahrain "Maungano ya bahari mbili." Maneno haya pia yanaonyesha ya kuwa *Israa* ya Nabii Musa ilikuwa ya njozi na ilikuwa safari ya roho, si ya kiwiliwili; maana dunia nzima hakuna mahali paitwapo *Majma'ul Bahrain.* Maneno haya yanaweza kuwa na maana moja tu, yaani, *Maungano ya bahari mbili.* Mahali pa namna hii, palipo karibu na mahali alipokaa Nabii Musa baada ya kutoka Misri, ni Baab-ul-Mandab, zinapoungana bahari ya Sham na Bahari ya Hindi; mahali pengine ni Milangobahari ya Dardanelles zinapoungana bahari ya Mediterraneo na bahari ya Marmora; na mahali pengine ni Al-Bahrain yanapokutana maji ya Ghuba ya Ajemi na Bahari ya Hindi. Katika mahali hapo pote, milangobahari ya Dardanelles tu ndipo panaweza kuwa mahali ambapo pangeweza kufanyika mkutano huo wa Nabii Musa na "Mtumishi wa Mungu"; maana njiani kuna nchi ya Kanaan alikokusudia kufika Nabii Musa, lakini akawahi kufariki kabla ya kufika huko. Mahali hapo pengine kila pamoja ni umbali wa maili elfu moja toka mahali alipokuwa Nabii Musa. Na kwa kuangalia hali za kusafiri katika zama hizo, ingemchukua Nabii Musa karibu mwaka mzima kufika huko. Na hali ya watu wake ilivyokuwa, asingeweza kuwaacha kwa muda mrefu namna hiyo kwa kuchelea wasielekee katika kufuru. Licha ya huu ushahidi wa nje wa historia, kuna ushahidi wa ndani pia, unaoonyesha ya kuwa safari hiyo ya Nabii Musa haikuwa ya kimwili, bali ya njozi:-

(a) Yule "mtaalamu" alitoboa safina ili kuifanya isichukuliwe na mfalme. Sasa swali ni hili, je jahazi lile lilisafiriwa baada ya kutobolewa au hapana? Kama lilisafiriwa, kwa nini mfalme asilikamate? Na kama halikusafiriwa kwa nini halikuzama? Katika huu ulimwengu hakuna chombo kinachojulikana kuendelea kuelea juu ya maji baada ya kutobolewa. Lakini katika ulimwengu wa njozi na ndoto hayo yanawezekana.

(b) Kuuawa kwa yule mtoto pia kunaonyesha habari hii ilikuwa ya njozi, maana hakuna mtu na akili zake, wacha mbali Nabii wa Mungu, angeweza kumwua mtu bila sababu za halali.

(c) Tukio la kujenga ukuta pia linaonyesha vivyo hivyo. Ingewezekanaje Nabii wa Mungu kama Musa, mtu ambaye ana moyo mkubwa na mawazo mapana, kumlaumu mwenziwe anapofanya jambo zuri la kuwajengea watu ukuta wao kwa sababu wenyeji wa mji ule walikataa kuwakaribisha?

62. Basi walipofika wote wawili (mahali) zinapoungana, wakamsahau samaki wao, naye akashika njia yake baharini kwa upesi.

فَلَمَّا بَلَغَا مَجْمَعَ بَيْنِهِمَا نَسِيَا حُوتَهُمَا فَاتَّخَذَ سَبِيلَهُ فِي الْبَحْرِ سَرَبًا ﴿٦٢﴾

63. Na walipofika mbele, (Musa) akamwambia kijana wake: Tupe chakula chetu; maana tumepata uchovu katika safari yetu hii.

فَلَمَّا جَاوَزَا قَالَ لِفَتَاهُ آتِنَا غَدَاءَنَا لَقَدْ لَقِينَا مِنْ سَفَرِنَا هَٰذَا نَصَبًا ﴿٦٣﴾

(d) Ibni Abbas anasimuliwa kusema ya kwamba neno kanz (hazina) linalotokea katika Aya 83 maana yake ni "hazina ya elimu." Habari hii inaonyesha ya kwamba neno hili limetumiwa katika Aya hiyo kwa maana ya mfano. Na kadhalika kuusimamisha ukuta na kuomba kukaribishwa hayakuwa mambo ya dhahiri, bali njozi.

Tamko la *Majma'ul-Bahrain* (Maungano ya bahari mbili) linaonyesha wakati wa kukoma Silsila ya Nabii Musa na kuanza Silsila ya Uislamu. Ta'tiir-ul-Anaam kinaeleza ya kwamba bahari inapoonekana katika njozi inaashiria mfalme mwenye nguvu na mwenye haki. Na pia inaonyesha kumsifu na kumtukuza Mungu. Kwa maana ya kwanza ya neno *bahr* (bahari) tamko la *Majma'ul-Bahrain* litakuwa na maana ya mkutano wa wafalme wawili wenye nguvu, haki na wema: yaani, Mtume Musa na Mtume Muhammad *s.a.w.;* na kwa maana ya pili tamko hilo litakuwa na maana ya Silsila mbili za dini - ya Musa na ya Kiislamu.

Tamko hili, *Au niendelee karne na karne,* linaonyesha ya kwamba Silsila ya Musa ilikuwa ya kuendelea kwa karne nyingi. Sheria ya Nabii Musa iliendelea kufanya kazi toka kufika yeye mwenyewe kwa miaka zaidi ya 2,000 mpaka alipofika Mtume Muhammad *s.a.w.* ikaanza Silsila mpya ya Kiislamu.

Aya 62. *Huut,* "Samaki" anapoonekana katika njozi, maana yake huwa nyumba za ibada za watu wacha-Mungu (Ta'tiir-ul-Anaam). Kwa maana hii maneno haya; *Walipofika wote wawili (mahali) zinapoungana, wakamsahau samaki wao,* yatakuwa na maana ya kwamba wakati zilipokutana kanuni ya Musa na ya Kiislamu, yaani kanuni ya Musa ilipokoma kufanya kazi, na ikaanza ya Kiislamu, ucha-Mungu wa kweli utawatoka wafuasi wa Musa na Yesu, na huo ucha-Mungu utakuwa alama maalum ya wafuasi wa dini mpya (sura 48:30). Kadhalika Aya hii inaonyesha ya kwamba Kanuni ya Kiislamu kwa hakika ni maendelezo tu ya Kanuni ya Musa, zikiwa sehemu mbili zinazofuatana za Mwongozo uliotoka kwa Allah.

Aya 63. Kuomba "chakula cha asubuhi" katika ndoto mradi wake ni "kuchoka" (Ta'tiir-ul-Anaam), Na Aya inakusudia kusema ya kwamba penye "maungano ya bahari mbili", yaani, atakapofika Mtume Muhammad *s.a.w.* wafuasi wa Musa na wa Yesu hawatamkubali. Wataendelea na safari yao peke yao na watakataa kukubali ya kuwa muda wa kufanya kazi Sheria yao umekwisha. Kisha baada ya kuendelea na safari hiyo kwa muda mrefu mpaka wachoke kumngoja Nabii Aliyeahidiwa (katika Kumbukumbu 18:18); hapo wataanza kustaajabu kama ni kweli kisha kuja nao wamekosa kumtambua, au namna gani? Katika Aya hii, Musa na kijana wake (Yesu) ni alama ya Mayahudi na Wakristo.

قَالَ اَرَءَيْتَ اِذْ اَوَيْنَاۤ اِلَى الصَّخْرَةِ فَاِنِّىْ نَسِيْتُ الْحُوْتَ ۖ وَمَاۤ اَنْسٰنِيْهُ اِلَّا الشَّيْطٰنُ اَنْ اَذْكُرَهٗ ۚ وَاتَّخَذَ سَبِيْلَهٗ فِى الْبَحْرِ ۖ عَجَبًا ﴿٦٤﴾

64. Akasema: Je, una habari, tulipopumzika penye mwamba, hapo nilimsahau samaki - na hakuna aliyenisahaulisha isipokuwa Shetani, nisikumbuke - naye akashika njia yake baharini kwa namna ya ajabu.

قَالَ ذٰلِكَ مَا كُنَّا نَبْغِ ۚ فَارْتَدَّا عَلٰۤى اٰثَارِهِمَا قَصَصًا ﴿٦٥﴾

65. (Musa) akasema: Hapo ndipo tulikuwa tunapataka. Basi wakarudi nyuma kwa kufuata nyayo zao.

فَوَجَدَا عَبْدًا مِّنْ عِبَادِنَاۤ اٰتَيْنٰهُ رَحْمَةً مِّنْ عِنْدِنَا وَعَلَّمْنٰهُ مِنْ لَّدُنَّا عِلْمًا ﴿٦٦﴾

66. Basi wakamkuta mtumishi katika watumishi Wetu Tuliyempa rehema kutoka Kwetu na Tuliyemwelimisha elimu kutoka Kwetu.

قَالَ لَهٗ مُوْسٰى هَلْ اَتَّبِعُكَ عَلٰۤى اَنْ تُعَلِّمَنِ مِمَّا عُلِّمْتَ رُشْدًا ﴿٦٧﴾

67. Musa akamwambia: Je, nikufuate ili unifundishe katika ule mwongozo uliofundishwa?

قَالَ اِنَّكَ لَنْ تَسْتَطِيْعَ مَعِىَ صَبْرًا ﴿٦٨﴾

68. Akasema: Hakika wewe huwezi kuvumilia kuwa pamoja nami.

وَكَيْفَ تَصْبِرُ عَلٰى مَا لَمْ تُحِطْ بِهٖ خُبْرًا ﴿٦٩﴾

69. Na unawezaje kuvumilia juu ya lile usilolizunguka elimu yake?

Aya 64. *Swakhra* "Mwamba" katika lugha ya ndoto na njozi maana yake ni "maisha ya uovu na dhambi." Hivyo maneno haya, *Tulipopumzika penye mwamba* yana maana ya kwamba, bahari mbili zitakapokutana, yaani, kukoma kwa Sheria ya Musa, na kufika kwa Mtume mpya na kuanza Sheria nyingine, basi Mayahudi na Wakristo watazama katika maisha ya dhambi na uovu.

Maneno haya, *Akashika njia yake baharini kwa namna ya ajabu,* yanaonyesha ya kwamba utawa wa kweli na ibada ya Allah vitawaacha watu hao na vitakuwa alama maalumu ya watu wengine (wafuasi wa dini ya Kiislamu) ambao watazirithi fadhili za Allah.

Hii habari ya samaki pia inaonyesha ya kuwa matokeo hayo yote yalikuwa ya njozi.

Aya 66. *Mtumishi* wa Mungu ambaye Nabii Musa alimfungia safari hii ya kumtafuta si mwingine ghairi ya Mtume Muhammad *s.a.w.* Roho ya Mtume *s.a.w.* ilipata umbo la mwili katika njozi ya Nabii Musa. Dalili zifuatazo zinaonyesha bila taabu ya kuwa Mtume Muhammad *s.a.w.* ndiye *'abd* anayetajwa katika kisa hiki:-

(a) Mtume Muhammad *s.a.w.* ameitwa *'abd* mahali pengi katika Qur'an (sura 2:24; 8:42; 17:2; 18:2; 25:2; 39:37; 53:11 na 72:20).

(b) Maneno haya, *Tuliyempa rehema,* ni wazi yanamhusu Mtume Muhammad *s.a.w.* Yeye peke yake ameitwa katika Qur'an "Rehema kwa walimwengu" (sura 21:108).

(c) Maneno, *Tuliyemwelimisha elimu kutoka Kwetu* pia yanamhusu Mtume s.a.w., mahali pengi katika Qur'an amesemwa amepewa elimu kwa kadiri kubwa sana (sura 4:114; 6:92; 20:115 na 27:7).

قَالَ سَتَجِدُنِيٓ إِن شَآءَ ٱللَّهُ صَابِرًا وَلَآ أَعۡصِي لَكَ أَمۡرٗا ٦٩

70. Akasema: Utanikuta mimi, Allah Akipenda, nikiwa mvumilivu na sitaasi amri yako.

قَالَ فَإِنِ ٱتَّبَعۡتَنِي فَلَا تَسۡـَٔلۡنِي عَن شَيۡءٍ حَتَّىٰٓ أُحۡدِثَ لَكَ مِنۡهُ ذِكۡرٗا ٧٠

71. Akasema: Basi kama utanifuata, usiniulize juu ya cho chote, mpaka mimi nianze kukuambia.

FUNGU 10

فَٱنطَلَقَا حَتَّىٰٓ إِذَا رَكِبَا فِي ٱلسَّفِينَةِ خَرَقَهَاۖ قَالَ أَخَرَقۡتَهَا لِتُغۡرِقَ أَهۡلَهَا لَقَدۡ جِئۡتَ شَيۡـًٔا إِمۡرٗا ٧١

72. Basi wote wawili wakaondoka, hata walipopanda safina (yule mtu) akaitoboa. (Musa) akasema: Je, umeitoboa ili uwazamishe waliomo? Hakika umefanya jambo lichukizalo.

قَالَ أَلَمۡ أَقُلۡ إِنَّكَ لَن تَسۡتَطِيعَ مَعِيَ صَبۡرٗا ٧٢

73. Akasema: Je, sikusema kuwa hakika wewe huwezi kuvumilia kuwa pamoja nami?

قَالَ لَا تُؤَاخِذۡنِي بِمَا نَسِيتُ وَلَا تُرۡهِقۡنِي مِنۡ أَمۡرِي عُسۡرٗا ٧٣

74. (Musa) akasema: Usinishike kwa yale niliyosahau, wala usinitie katika taabu kwa jambo langu (hili).

Aya 70. Aya hii pia inaonyesha ya kuwa habari hii ilikuwa ya njozi. Maana Nabii Musa alikuwa Mtume aliyejitegemea, na Kiongozi mkubwa wa watu wake na Manabii wengi walifika kufuata na kuendeleza Silsila yake. Hivyo katika mambo ya Sheria, ingekuwa hayo ni matokeo ya dhahiri, asingekuwa na haja ya kumtii au kufundishwa na mtu ye yote. Kadhalika Aya hii inaonyesha ya kwamba wafuasi wa Musa watalazimika kumfuata Mtume *s.a.w.* atakapofika. Na hii ndiyo sababu Mtume *s.a.w.* akasema; "Kama Musa na Isa wangekuwa hai, wasingelikuwa na njia ila kunifuata" (Kathir jalada 11, uk. 246).

Aya 72. *Safina* katika lugha ya ndoto mradi wake ni "utajiri wa kidunia." Tafsiri hii pia inatiwa nguvu na Qur'an (sura 17:67). Kwa maana hii, Musa na mwenziwe mtaalamu kuingia jahazini, maana yake ni kwamba wafuasi wa Musa na wa Mtume *s.a.w.* wote watapata utajiri katika nyakati zao.

Neno hili, *akaitoboa,* linaonyesha ya kwamba Mtume Muhammad *s.a.w.* atatia tundu katika mali na mafanikio ya wafuasi wake; yaani ataangalia ya kwamba mali yasilundikane katika mikono ya watu wachache; bali yaendelee kutembea baina ya watu na yagawanyike vizuri kati ya watu wote. Kutimiza jambo hili, Islam imeweka kanuni ya lazima ya kutoa Zaka; imekataza kabisa riba; imeweka sheria ya urithi inayofanya mali ienee kwa watu wengi; imekataza kucheza kamari na imeweka kanuni za kutengeneza hali za vibarua kuwa njema. Mayahudi na Wakristo hawapendelei kanuni hizi na wanaziona kuwa uharibifu usiyo na akili. Kanuni zao zote zinaelekea kuuzidisha utajiri wa matajiri na kuifanya mali ikusanyike katika mikono ya watu wachache. Nabii Musa kulaumu njozini kutobolewa kwa jahazi ile, maana yake ni kuwa watu wake hawatakubali kuweka kanuni za kufanya mali iingie katika mikono ya watu wengi. Mtume s.a.w. katika Njozi yake alikataa kikombe cha maji aliyopewa, ambayo maana yake ni kuwa wafuasi wake watapendelea dini kuliko dunia.

75. Basi wote wawili wakaendelea, hata wakamkuta kivulana, na (yule mtu) akamwua. (Musa) akasema: Je, umemwua mtu asiye na kosa wala hakumwua mtu? Bila shaka umefanya jambo baya!

فَانْطَلَقَا ۫ حَتّٰٓى اِذَا لَقِيَا غُلٰمًا فَقَتَلَهٗ ۙ قَالَ اَقَتَلْتَ نَفْسًا زَكِيَّةًۢ بِغَيْرِ نَفْسٍ ؕ لَقَدْ جِئْتَ شَيْـًٔا نُّكْرًا ﴿٧٥﴾

JUZU 16

76. (Mtu yule) akasema: Je, sikukuambia: Hakika wewe huwezi kuvumilia kuwa pamoja nami?

قَالَ اَلَمْ اَقُلْ لَّكَ اِنَّكَ لَنْ تَسْتَطِيْعَ مَعِيَ صَبْرًا ﴿٧٦﴾

77. (Musa) akasema: Nikikuuliza juu ya cho chote baada ya haya, basi usinifanye sahibu; maana umekwisha pata kwangu udhuru.

قَالَ اِنْ سَاَلْتُكَ عَنْ شَيْءٍۢ بَعْدَهَا فَلَا تُصٰحِبْنِيْ ۚ قَدْ بَلَغْتَ مِنْ لَّدُنِّيْ عُذْرًا ﴿٧٧﴾

78. Basi wakaendelea hata walipowafikia watu wa mji, wakawaomba wenyeji wake chakula, lakini wakakataa kuwakaribisha, Wakakuta humo ukuta unataka kuanguka, na (yule mtu) akausimamisha. (Musa) akasema: Kama ungetaka, bila shaka ungeichukulia (kazi hii) ujira.

فَانْطَلَقَا ۫ حَتّٰٓى اِذَآ اَتَيَآ اَهْلَ قَرْيَةِ ِۨ اسْتَطْعَمَآ اَهْلَهَا فَاَبَوْا اَنْ يُّضَيِّفُوْهُمَا فَوَجَدَا فِيْهَا جِدَارًا يُّرِيْدُ اَنْ يَّنْقَضَّ فَاَقَامَهٗ ؕ قَالَ لَوْ شِئْتَ لَتَّخَذْتَ عَلَيْهِ اَجْرًا ﴿٧٨﴾

Aya 75. *Kivulana* katika ndoto mradi wake huwa ujinga, nguvu na kupenda starehe za kimwili na mengineyo. Yule mtaalamu kumwua kivulana yule katika njozi, na Nabii Musa kumlaumu, inaonyesha ya kwamba Uislamu utawataka wafuasi wake waue matamanio yao na shauku zao na kuzizuia kabisa tamaa zao za kimwili; lakini Mayahudi na Wakristo wapendao raha watalaumu amri hizo za Uislamu.

Neno *Fantalaqaa* (wakaendelea) ambalo limetumiwa mara kwa mara katika Aya hizi ni lile lile alilolitumia Malaika Jibrili katika Njozi ya Mtume *s.a.w.* ya *Israa: intalaq, intalaq* yaani, endelea, endelea.

Maneno haya *hata wakamkuta kivulana, na (yule mtu) akamwua,* pia yanaweza kuhusu kuuawa kwa adui mkuu wa Uislamu, Ka'b bin Ashraf, kiongozi wa machafuko kati ya Mayahudi waovu wa Madina ambaye aliuawa na kikundi cha Waislamu (Hisham).

Aya 77. Aya hii inaonyesha ya kwamba wafuasi wa Nabii Musa - Mayahudi - mara kwa mara watavunja mapatano yao na Mtume *s.a.w.* mpaka ujamaa baina yao na Mtume *s.a.w.* utavunjika kabisa.

Aya 78. Maneno *Ahlu qaryah* (watu wa mji) katika ndoto yanabashiri taifa moja au zaidi; na kuwaomba wakukaribishe, maana yake ni kuwataka msaada katika kazi njema. Katika maana

79. (Yule mtu) akasema: Hii ndiyo faraka baina ya mimi na wewe. Hivi sasa nitakuambia hakika ya yale ambayo hukuweza kuyavumilia.

قَالَ هٰذَا فِرَاقُ بَيْنِيْ وَبَيْنِكَ ۚ سَاُنَبِّئُكَ بِتَاْوِيْلِ مَا لَمْ تَسْتَطِعْ عَّلَيْهِ صَبْرًا ﴿٧٩﴾

80. Ama safina, basi ilikuwa ya maskini wafanyao kazi baharini; na nilitaka kuiharibu, na nyuma yao kulikuwa mfalme aliyekamata kila safina kwa nguvu.

اَمَّا السَّفِيْنَةُ فَكَانَتْ لِمَسٰكِيْنَ يَعْمَلُوْنَ فِي الْبَحْرِ فَاَرَدْتُّ اَنْ اَعِيْبَهَا وَكَانَ وَرَآءَهُمْ مَّلِكٌ يَّاْخُذُ كُلَّ سَفِيْنَةٍ غَصْبًا ﴿٨٠﴾

hii ya maneno *ahlu qaryah,* Aya italeta maana ya kwamba Nabii Musa na Mtume *s.a.w.* watataka msaada wa Mayahudi na Wakristo katika kazi ya Allah, lakini wote wawili watanyimwa msaada huo. Jinsi Mayahudi walivyokataa kumsaidia Nabii Musa inaonekana walipokataa kwenda naye kuishinda nchi ya Kanaan, kama inavyoonyeshwa na Qur'an (sura 5:22-25). Mtume *s.a.w.* pia hakuweza kupata msaada wa Wakristo ingawa katika jambo la maana sana la kusimamisha Umoja wa Allah duniani. Qur'an inasema, *Sema: Enyi watu wa Kitabu, njooni kwenye neno lililo sawa baina yetu na baina yenu, ya kwamba tusimwabudu ye yote ila Allah, wala tusimshirikishe na cho chote, wala baadhi yetu wasifanye wengine kuwa waungu badala ya Allah; lakini wakigeuka, basi semeni: Shuhudieni ya kwamba sisi ni Waislamu* (sura 3:65).

Kwa maelezo ya Ta'tiir-ul-Anaam, *jidaar* (ukuta) katika ndoto ukiwa na ufa, mradi wake ni kiongozi wa watu au mwanazuoni ambaye amepoteza mali yake; na kuutengeneza, inaonyesha kiongozi kurejewa na Mali yake.

Kwa mujibu wa tafsiri hii, maneno haya, *Na wakakuta humo ukuta unataka kuanguka,* yanaonyesha ya kwamba utafika wakati viongozi wa Mayahudi na Wakristo hawatakuwa na nguvu juu ya wafuasi wao; na kuuimarisha ukuta maana yake ni kwamba nguvu ile itawarudia. Maneno haya pia yanaweza kuhusu maendeleo waliyopata Waisraeli kwa kumfuata Musa, na waliyopata Waismaili kwa kumfuata Mtume *s.a.w.*

Maneno haya, *Kama ungetaka, bila shaka ungeichukulia (kazi hii) ujira,* yanaweza kuwa na maana ya kwamba silika ya uchumi ya Mayahudi itakuwa kubwa sana hata hawatakuwa tayari kufanya cho chote bila kutaka ujira.

Aya 79. Mtumishi wa Allah alipoona ya kuwa Musa, yaani wafuasi wake, ingawa amejaribu sana kuwataka wasaidie kueneza mafundisho ambayo yeye na wao wameshirikiana, lakini wameendelea tu kujiweka kando, akatambua ya kwamba italazimu atengane nao.

Aya 80. Katika Aya hii yanaanza maelezo ya matukio yaliyopita yaliyotolewa na Mtumishi wa Mwenyezi Mungu wa njozi ya Nabii Musa.

Neno 'maskini' linaonyesha watu wenye mioyo safi ambao mali mengi na ustawi haviwazuilii kuwaangalia wenye dhiki na wanyonge na kuchanganyika nao. Neno 'mfalme' linaonyesha upendo wa dunia. Hivyo, Aya hii inaonyesha ya kwamba watu wenye kiburi na majivuno wasiotaka kutumia mali zao kwa kuwahurumia watu, na ambao wamezama katika kuipenda dunia, wao wanakuwa windo jepesi la Shetani. Hii ndiyo sababu Mtume *s.a.w.* alitoboa jahazi la watu wake - akaweka sheria za namna ya kwamba pendo lao juu ya dunia hii litobolewe na pendo la Akhera, ili watumie mali zao kwa kuwafaa wanaoonewa na kudhalilishwa, na badala ya kutakabari juu yao, wao wawatumikie na kuwahurumia.

81. Na ama kivulana, basi wazazi wake walikuwa waaminio, na tukahofia kwamba asije kuwahangaisha kwa uasi na kufuru.

وَاَمَّا الْغُلٰمُ فَكَانَ اَبَوٰهُ مُؤْمِنَيْنِ فَخَشِيْنَآ اَنْ يُّرْهِقَهُمَا طُغْيَانًا وَّكُفْرًا ﴿٨٠﴾

82. Basi tulitaka ya kwamba Mola wao Awabadilishie aliye bora kuliko yeye kwa kutakasika na aliye karibu zaidi kwa huruma.

فَاَرَدْنَآ اَنْ يُّبْدِلَهُمَا رَبُّهُمَا خَيْرًا مِّنْهُ زَكٰوةً وَّاَقْرَبَ رُحْمًا ﴿٨١﴾

83. Na ama ukuta, basi ulikuwa wa watoto wawili mayatima mjini, na chini yake kulikuwa hazina yao, na baba yao alikuwa mwema; kwahiyo Mola wako

وَاَمَّا الْجِدَارُ فَكَانَ لِغُلٰمَيْنِ يَتِيْمَيْنِ فِى الْمَدِيْنَةِ وَكَانَ تَحْتَهٗ كَنْزٌ لَّهُمَا وَكَانَ اَبُوْهُمَا صَالِحًا ۚ فَاَرَادَ رَبُّكَ اَنْ يَّبْلُغَآ

Inafaa kuona ya kwamba katika njozi ya Mtume *s.a.w.,* pendo la dunia lilikuwa na umbo la mwanamke kizee; ilhali katika njozi ya Musa, pendo la dunia likachukua umbo la mfalme katili. Jambo hili laonyesha ya kwamba pendo la dunia halitatiliwa nguvu sana na wafuasi wa Mtume *s.a.w.* kama litakavyokuwa la kishindo upande wa Mayahudi na Wakristo.

Aya 81. Kama ilivyoonyeshwa katika Aya 75, *ghulaam* (kivulana) katika njozi mradi wake ni shughuli au wepesi, ukunjufu na matumaini, nguvu na ujinga; neno *qatala* (kuua) lina maana ya kupunguza nguvu au kuzima ukali wa kitu. Kwa maana hii, kumwua kivulana mradi wake utakuwa kupunguza matokeo mabaya ya ujinga na nguvu zipitazo kiasi na matumaini yasiyo na mpaka.

Neno *abawaahu* (wazazi wake) hapa mradi wake ni mwili na roho ya kibinadamu, kwa sababu wazazi au chanzo kinachozalisha tabia njema ni mwunganiko wa mwili wa kibinadamu na roho, ambavyo ni mtu binafsi yake. Hivyo kumwua kivulana katika njozi, mradi wake ni kuyatiisha na kuyatawala matamanio makali ya kibinadamu na kupunguza nguvu yao. Hivyo yule Mtumishi wa Mungu kumwua kivulana ili asiwasumbue wazazi wake kwa kufuru na uasi, kama ilivyoonekana katika njozi ya Musa, inaonyesha ya kwamba mwanadamu amepewa nguvu nyingi za kumwezesha kufanya vitendo vitukufu kabisa vya wema; na ili kuziwezesha nguvu hizo zifanye kazi, vipawa vya shughuli, uwezo na ujinga vimetiwa ndani ya mwanadamu. Mwanadamu anaweza kutimiza kusudi kubwa la kuumbwa kwake kwa kutumia nguvu hizo zinazotokana na mchanganyiko wa mwili na roho ya kibinadamu. Lakini kama nguvu hizo hazitatawaliwa vizuri, basi zitampeleka mtu kwenye uasi na kufuru. Nguvu hizi zimetiishwa na kupunguzwa kasi kwa amri na sheria ambazo Allah amemteremshia Mtume Muhammad *s.a.w.* kama inavyoonyeshwa katika kumwua kwake kivulana katika njozi ya Musa.

Aya 82. Mradi wa Aya hii ni kwamba Islam imeweka kanuni za sheria ili mwanadamu awezeshwe kuzitawala kabisa tamaa zake na hivyo afaidi maisha mapya ya kiroho. Lakini kama ilivyoelezwa juu wafuasi wa Nabii Musa walijiendekeza katika matamanio yao hafifu, wakijiweka katika maisha ya raha na starehe, wakaruka mipaka yote ya kiasi na busara.

Aya 83. Kama ilivyokwisha elezwa, neno *jidaar* (ukuta) mradi wake ni wakubwa wa Mayahudi, yaani Nabii Musa na Nabii Isa (Aya 78) na Nabii Ibrahimu.

Alitaka wafikie balehe yao na wajitolee hazina yao; ni rehema kutoka kwa Mola wako; nami sikulifanya kwa amri yangu. Hiyo ndiyo katika yale ambayo hukuweza kuyavumulia.

اَشُدَّهُمَا وَيَسْتَخْرِجَا كَنْزَهُمَا ۖ رَحْمَةً
مِّنْ رَّبِّكَ ۚ وَمَا فَعَلْتُهٗ عَنْ اَمْرِىْ ۭ ذٰلِكَ
تَاْوِيْلُ مَا لَمْ تَسْطِعْ عَّلَيْهِ صَبْرًا ۝٨٢ ع

Neno *kanz* (hazina) maana yake ni hazina ya elimu ya kiungu waliyopewa Nabii Musa na Nabii Isa.

Aya inakusudia kusema ya kwamba Allah amehifadhi katika Qur'an hazina kubwa ya elimu ya kiroho waliyopewa Musa na Isa (sura 98:4) ambayo ilikuwa katika hatari ya kupotea kwa sababu ya kupuuza dini kwa Mayahudi na kuzamilia kwao mambo ya kidunia; ili watakapokuja kuitambua haki, waipokee.

Maneno haya, *Rehema kutoka kwa Mola wako,* maana yake ni kwamba Allah kuihifadhi sehemu isiyobatilika ya mafundisho ya Musa na Isa katika Qur'an ni tendo la huruma Yake, maana Mayahudi, kwa kuasi kwao mara kwa mara, walikuwa wamejinyima haki ya kupewa rehema ya Allah. Lakini licha ya fedhuli yao, Allah aliwahurumia kwa kuihifadhi hazina yao ya elimu ya kiroho katika Qur'an kwa ajili ya kuongoka kwao.

Maneno haya, *Nami sikulifanya kwa amri yangu,* maana yake ni kwamba kazi ya kuihifadhi hazina ile ya elimu ya kiungu ni ya Allah Mwenyewe, na Mtume *s.a.w.* hakuwa na shauri ndani yake. Jambo hili pia limetajwa katika sura 53:4 pasemapo, *Wala hasemi kwa tamaa ya nafsi yake.*

Baada ya kusoma matokeo yaliyotajwa katika Aya zilizopita pamoja na maelezo yao, inakuwa wazi kabisa ya kuwa njozi ya Nabii Musa imetajwa hapa kuonyesha mambo haya yafuatayo:-

(1) Ilikadiriwa na ndivyo ilikuwa sawa ya kwamba Mtume Muhammad *s.a.w.* adhihiri wakati Wakristo - ambao ndiyo sehemu ya pili ya Silsila ya Musa - watakapokuwa wameharibika.

(2) Kwa kuwa mafundisho ya Kiislamu yalisimamishwa juu ya kanuni na sheria zilizohitilafiana na Sheria ya Musa, kusaidiana halisi baina ya Mayahudi na Waislamu kulikuwa hakuwezekani; lakini pia kuokoka bila kufuata mafundisho ya Kiislamu ni jambo lisilowezekana.

(3) Mayahudi na Wakristo watakataa kumkubali Mtume Muhammad *s.a.w.* nao watafuata njia zao zilizo mbalimbali, lakini mwishoni watalazimika kumtii.

(4) Baada ya safari yao ndefu na ya uchovu, na baada ya kukata tamaa ya kupata amani ya kweli na utulivu wa mioyo kwa kutegemea juhudi zao zisizokuwa na msaada wa Allah, Mayahudi na Wakristo watalazimika kujirudi na kufikiria hali yao; nao watatambua ya kwamba kwa kuwa dini yao imechakaa toka siku nyingi, iliwapasa kuiachilia mbali toka hapo hapo kwanza.

(5) Baada ya kuwafunukia jambo hili, bishara zinazowahusu zilizohifadhiwa katika Qur'an zitawaongoza Mayahudi na Wakristo kumkubali Mtume Muhammad *s.a.w*.

(6) Baada ya kuukubali Uislamu, watatii sheria na vipimo ulivyoviweka vya kuongoza mwenendo wa wanadamu, na kwa kuzizuia tamaa zao watajisalimisha kwenye amri ya Allah, na hivyo watajivutia rehema za Allah, nao wataogelea katika bahari ya rehema Zake.

Kwa hakika *Israa* ya Nabii Musa ilikuwa kitangulizi kizuri cha kufika Silsila ya Uislam iliyokuja kuiondoa Silsila ya dini ya Musa.

FUNGU 11

84. Na wanakuuliza habari za Dhul-Karnain. Sema: Kwa yakini nitawasomeeni katika hadithi yake.

وَيَسْـَٔلُوْنَكَ عَنْ ذِى الْقَرْنَيْنِ ؕ قُلْ
سَاَتْلُوْا عَلَيْكُمْ مِّنْهُ ذِكْرًا ﴿٨٤﴾

85. Bila shaka Tulimwimarisha katika ardhi, na Tukampa njia za kupatia kila kitu.

اِنَّا مَكَّنَّا لَهٗ فِى الْاَرْضِ وَاٰتَيْنٰهُ مِنْ
كُلِّ شَىْءٍ سَبَبًا ﴿٨٥﴾

86. Ndipo akaifuata njia.

فَاَتْبَعَ سَبَبًا ﴿٨٦﴾

87. Mpaka alipofika machweo ya jua akaliona linatua katika chemchem iliyovurugika, na pale akawakuta watu, Tukasema: Ewe Dhul-Karnain, Uwaadhibu au uwafanyie wema.

حَتّٰٓى اِذَا بَلَغَ مَغْرِبَ الشَّمْسِ وَجَدَهَا
تَغْرُبُ فِىْ عَيْنٍ حَمِئَةٍ وَّوَجَدَ عِنْدَهَا
قَوْمًا ؕ قُلْنَا يٰذَا الْقَرْنَيْنِ اِمَّآ اَنْ تُعَذِّبَ
وَاِمَّآ اَنْ تَتَّخِذَ فِيْهِمْ حُسْنًا ﴿٨٧﴾

88. Akasema: Ama anayedhulumu basi bila shaka tutamwadhibu; kisha atarudishwa kwa Mola wake, naye Atamwadhibu adhabu kali.

قَالَ اَمَّا مَنْ ظَلَمَ فَسَوْفَ نُعَذِّبُهٗ ثُمَّ
يُرَدُّ اِلٰى رَبِّهٖ فَيُعَذِّبُهٗ عَذَابًا نُّكْرًا ﴿٨٨﴾

89. Waama mwenye kuamini na kufanya vitendo vizuri, basi atapata ujira mwema; nasi Tutamwambia lililo rahisi katika amri Yetu.

وَاَمَّا مَنْ اٰمَنَ وَعَمِلَ صَالِحًا فَلَهٗ جَزَآءَ ۨ
الْحُسْنٰى ۚ وَسَنَقُوْلُ لَهٗ مِنْ اَمْرِنَا يُسْرًا ﴿٨٩﴾

Aya 84. *Dhul-Qarnain.* Maelezo ya Qur'an juu ya huyu Dhul-Karnain yanapatana sana na habari za mfalme Cyrus aliyetawala nchi ya Ajemi baada ya kifo cha baba yake, na baadaye akaishinda Media ambayo ilikuwa ufalme mkubwa kuliko Ajemi yenyewe. Qur'an imeonyesha alama nne za huyu Dhul-Karnain: (1) Alikuwa Mtumishi mtawa wa Allah na alikuwa akipokea wahyi (ufunuo) (Aya 87, 92 na 99). (2) Alikuwa mshindi mkuu wa vita na mtawala mwema mwenye haki; na mataifa aliyoyashinda akayatendea kwa ukarimu kabisa (Aya 85, 89). (3) Alikwenda upande wa magharibi na akashinda vita sana mpaka alipofika mahali akaona jua linatua ndani ya chemchem ya maji yaliyovurugika, kisha akaelekea upande wa Mashariki na akashinda nchi nyingi (Aya 85, 87, 88, 89). (4) Mwisho akaenda sehemu za katikati ambako kulikaa washenzi, na ambako Gog na Magog (Yajuja na Majuja) walikuwa wakishambulia, na akajenga ukuta kuzuia mashambulio hayo (Aya 94-98). Sasa katika wafalme wakubwa wa zamani Cyrus ndiye anazo sifa hizo nne kwa wingi kabisa. Hivyo, yeye anastahili kufikiriwa kuwa Dhul-Karnain anayeelezwa na Qur'an.

Aya 85. *Kila kitu,* mradi wake ni kila kitu kilichohitajiwa kwa kumalizia kazi yake.

Aya 87. Maneno haya, *Akaliona linatua katika chemchem iliyovurugika,* yanaonyesha ya kwamba maji yale yalikuwa mapana sana, yaani bahari. hata inakuwa ukisimama pwani wakati wa magharibi jua linaonekana linatua ndani ya bahari. Bahari hiyo inaitwa Bahari nyeusi iliyoko Asia Minor.

ثُمَّ اَتۡبَعَ سَبَبًا ﴿۹۰﴾

90. Kisha akaifuata njia.

حَتّٰۤى اِذَا بَلَغَ مَطۡلِعَ الشَّمۡسِ وَجَدَهَا تَطۡلُعُ عَلٰى قَوۡمٍ لَّمۡ نَجۡعَلۡ لَّهُمۡ مِّنۡ دُوۡنِهَا سِتۡرًا ﴿۹۱﴾

91. Hata alipofika maawio ya jua, akaliona linawatokea watu Tusio-wawekea pazia la kuwakinga nalo.

كَذٰلِكَ ؕ وَقَدۡ اَحَطۡنَا بِمَا لَدَيۡهِ خُبۡرًا ﴿۹۲﴾

92. Ni kama hivyo. Na Tulikuwa Tumezizunguka habari zilizokuwa pamoja naye.

ثُمَّ اَتۡبَعَ سَبَبًا ﴿۹۳﴾

93. Kisha akaifuata njia

حَتّٰۤى اِذَا بَلَغَ بَيۡنَ السَّدَّيۡنِ وَجَدَ مِنۡ دُوۡنِهِمَا قَوۡمًا ۙ لَّا يَكَادُوۡنَ يَفۡقَهُوۡنَ قَوۡلًا ﴿۹۳﴾

94. Hata alipofika katikati ya milima miwili, akakuta watu nyuma yao ambao waliweza kwa shida kufahamu neno.

قَالُوۡا يٰذَا الۡقَرۡنَيۡنِ اِنَّ يَاۡجُوۡجَ وَمَاۡجُوۡجَ مُفۡسِدُوۡنَ فِى الۡاَرۡضِ فَهَلۡ نَجۡعَلُ لَكَ خَرۡجًا عَلٰۤى اَنۡ تَجۡعَلَ بَيۡنَنَا وَبَيۡنَهُمۡ سَدًّا ﴿۹۴﴾

95. Walisema: Ewe Dhul-Karnain! hakika Yajuja na Majuja wanafanya uharibifu katika ardhi, basi je, tukupe kodi kwa sharti utie baina yetu na baina yao kizuizi?

قَالَ مَا مَكَّنِّىۡ فِيۡهِ رَبِّىۡ خَيۡرٌ فَاَعِيۡنُوۡنِىۡ بِقُوَّةٍ اَجۡعَلۡ بَيۡنَكُمۡ وَبَيۡنَهُمۡ رَدۡمًا ﴿۹۵﴾

96. Akasema: Yale ambayo kwayo Mola wangu Ameniimarisha ni bora; lakini nisaidieni kwa nguvu, nitaweka baina yenu na baina yao kizuizi.

اٰتُوۡنِىۡ زُبَرَ الۡحَدِيۡدِ ؕ حَتّٰۤى اِذَا سَاوٰى بَيۡنَ الصَّدَفَيۡنِ قَالَ انۡفُخُوۡا ؕ حَتّٰۤى اِذَا جَعَلَهٗ نَارًا ۙ قَالَ اٰتُوۡنِىۡۤ اُفۡرِغۡ عَلَيۡهِ قِطۡرًا ﴿۹۶﴾

97. Nileteeni vipande vya chuma. Hata alipoijaza nafasi katikati ya milima miwili, akasema: Fukuteni (moto), mpaka alipokifanya kuwa (kama) moto, akasema: Nileteeni shaba iliyoyeyuka nikimwagie.

فَمَا اسۡطَاعُوۡۤا اَنۡ يَّظۡهَرُوۡهُ وَمَا اسۡتَطَاعُوۡا لَهٗ نَقۡبًا ﴿۹۷﴾

98. Basi (Yajuja na Majuja) hawakuweza kuukwea wala hawakuweza kuutoboa.

قَالَ هٰذَا رَحۡمَةٌ مِّنۡ رَّبِّىۡ ۚ فَاِذَا جَآءَ وَعۡدُ رَبِّىۡ جَعَلَهٗ دَكَّآءَ ۚ وَكَانَ وَعۡدُ رَبِّىۡ حَقًّا ﴿۹۸﴾

99. Akasema: Hii ni rehema itokayo kwa Mola wangu; na itakapofika ahadi ya Mola wangu, Atauvunja-vunja. Na ahadi ya Mola wangu ni kweli.

Aya 99. Maneno haya, *Hii ni rehema itokayo kwa Mola wangu,* yanaonyesha unyenyekevu na ucha-Mungu wa Cyrus. Kama alivyo Mtumishi mtawa wa Mungu, hakujitapa kwa kushinda nchi nyingi, bali akasema yote yale ni rehema ya Mungu.

وَتَرَكْنَا بَعْضَهُمْ يَوْمَئِذٍ يَّمُوْجُ فِيْ بَعْضٍ وَّنُفِخَ فِي الصُّوْرِ فَجَمَعْنٰهُمْ جَمْعًا ﴿٩٩﴾

100. Na Tutawaacha baadhi yao siku hiyo wakiwasonga wengine, na itapulizwa baragumu, ndipo Tutawakusanya wote pamoja.

وَّعَرَضْنَا جَهَنَّمَ يَوْمَئِذٍ لِّلْكٰفِرِيْنَ عَرْضًا ﴿١٠٠﴾

101. Na Tutaileta Jahanamu siku hiyo mbele ya makafiri ana kwa ana,

الَّذِيْنَ كَانَتْ اَعْيُنُهُمْ فِيْ غِطَآءٍ عَنْ ذِكْرِيْ وَكَانُوْا لَا يَسْتَطِيْعُوْنَ سَمْعًا ﴿١٠١﴾

102. Ambao macho yao yalikuwa katika pazia yasijali mawaidha Yangu, na walikuwa hawawezi kusikia.

FUNGU 12

اَفَحَسِبَ الَّذِيْنَ كَفَرُوْٓا اَنْ يَّتَّخِذُوْا عِبَادِيْ مِنْ دُوْنِيْٓ اَوْلِيَآءَ ؕ اِنَّآ اَعْتَدْنَا جَهَنَّمَ لِلْكٰفِرِيْنَ نُزُلًا ﴿١٠٢﴾

103. Je, waliokufuru wanadhani ya kwamba watawashika watumishi Wangu kuwa walinzi badala Yangu? Hakika Sisi Tumeiandaa Jahanamu iwe karamu kwa makafiri.

قُلْ هَلْ نُنَبِّئُكُمْ بِالْاَخْسَرِيْنَ اَعْمَالًا ؕ ﴿١٠٣﴾

104. Sema, " Je Tuwaambieni wale wenye hasara zaidi kuhusiana na vitendo vyao?

اَلَّذِيْنَ ضَلَّ سَعْيُهُمْ فِي الْحَيٰوةِ الدُّنْيَا وَهُمْ يَحْسَبُوْنَ اَنَّهُمْ يُحْسِنُوْنَ صُنْعًا ﴿١٠٤﴾

105. Ni ambao bidii yao imepotea katika maisha ya dunia, nao wanafikiri kwamba wanazifanya vema sanaa.

اُولٰٓئِكَ الَّذِيْنَ كَفَرُوْا بِاٰيٰتِ رَبِّهِمْ وَلِقَآئِهٖ فَحَبِطَتْ اَعْمَالُهُمْ فَلَا نُقِيْمُ لَهُمْ يَوْمَ الْقِيٰمَةِ وَزْنًا ﴿١٠٥﴾

106. Hao ndio waliozikataa Ishara za Mola wao na kukutana naye. Kwa hiyo vitendo vyao vimeharibika, wala hatutawasimamishia mizani siku ya Kiyama.

ذٰلِكَ جَزَآؤُهُمْ جَهَنَّمُ بِمَا كَفَرُوْا وَاتَّخَذُوْٓا اٰيٰتِيْ وَرُسُلِيْ هُزُوًا ﴿١٠٦﴾

107. Hiyo Jahanamu ni malipo yao kwa sababu walikufuru na kuzifanyia mzaha Ishara Zangu na Mitume wangu.

اِنَّ الَّذِيْنَ اٰمَنُوْا وَعَمِلُوا الصّٰلِحٰتِ كَانَتْ لَهُمْ جَنّٰتُ الْفِرْدَوْسِ نُزُلًا ﴿١٠٧﴾

108. Kwa yakini walioamini na kufanya vitendo vizuri kao lao litakuwa bustani za Peponi.

Aya 103. Aya hii inaeleza habari za watu wanaomfanya Yesu kuwa mwokozi wao na kuwa mwana wa Mungu, na ambao habari zao zilianza kutajwa mwanzo wa sura hii. Jambo hili linaonyesha ya kuwa Aya zilizotangulia pia zinaeleza habari za watu hawa hawa - Wakristo wa Magharibi.

خٰلِدِيْنَ فِيْهَا لَا يَبْغُوْنَ عَنْهَا حِوَلًا ﴿١٠٨﴾

109. Watakaa humo; hawatataka mabadiliko kutoka humo.

قُلْ لَّوْ كَانَ الْبَحْرُ مِدَادًا لِّكَلِمٰتِ رَبِّيْ لَنَفِدَ الْبَحْرُ قَبْلَ اَنْ تَنْفَدَ كَلِمٰتُ رَبِّيْ وَلَوْ جِئْنَا بِمِثْلِهٖ مَدَدًا ﴿١٠٩﴾

110. Sema: Kama bahari ingalikuwa wino kwa (kuyaandika) maneno ya Mola wangu, bila shaka bahari ingalikwisha kabla ya kwisha maneno ya Mola wangu, ingawa Tungalileta (bahari) kama hiyo kuongezea.

قُلْ اِنَّمَآ اَنَا بَشَرٌ مِّثْلُكُمْ يُوْحٰٓى اِلَيَّ اَنَّمَآ اِلٰهُكُمْ اِلٰهٌ وَّاحِدٌ ۚ فَمَنْ كَانَ يَرْجُوْا لِقَآءَ رَبِّهٖ فَلْيَعْمَلْ عَمَلًا صَالِحًا وَّلَا يُشْرِكْ بِعِبَادَةِ رَبِّهٖٓ اَحَدًا ﴿١١٠﴾ ع ١٢

111. Sema: Bila shaka mimi ni binadamu kama ninyi; inafunuliwa kwangu ya kwamba Mungu wenu ni Mungu Mmoja tu. Basi anayetumaini kukutana na Mola wake, na afanye vitendo vizuri wala asimshirikishe ye yote katika ibada ya Mola wake.

Aya 111. Hapa Mtume *s.a.w.* anaamrishwa awaambie Wakristo wasioamini ya kuwa ingawa amekwisha bashiri siri nyingi juu ya ushindi wa dini ya Kiislamu na kuanguka kwa mataifa ya Kikristo, hata hivyo hawezi kudai kuwa yeye ni mwana wa Mungu au anazo nguvu za kiungu. Yeye ni mwanadamu tu, na sifa yake iko katika kuleta ujumbe wa Allah, basi waache kumshirikisha na miungu ya uwongo.

Imesimuliwa ya kuwa Mtume *s.a.w.* alisema, Kusoma Aya kumi za mwisho na za mwanzo wa sura hii kunamlinda mtu na mashambulio ya kiroho ya *Dajjaal*. Hii inaonyesha ya kuwa *Dajjaal* na *Yaajuuj* na *Maajuuj* si wengine ila ni haya mataifa ya Wakristo ya Magharibi. Neno *Dajjaal* linaonyesha hali mbaya ya dini yao, na *Yaajuuj* na *Maajuuj* yanaonyesha hali ya nguvu yao katika mambo ya utawala.

سُوْرَةُ مَرْيَمَ مَكِّيَّةٌ وَّ هِيَ مَعَ الْبَسْمَلَةِ تِسْعٌ وَّ تِسْعُوْنَ اٰيَةً وَّ سِتَّةُ رُكُوْعَاتٍ

19. SURA MARYAM

Imeteremshwa Makka

Ina mafungu 6 na Aya 99 pamoja na Bismillahi

بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ ①

1. Kwa jina la Allah, Mwingi wa rehema, Mwingi wa ukarimu.

كٓهٰيٰعٓصٓ ②

2. (Allah ni) Mkarimu, Mwongozi, Mzima wa milele, Mkuu, Mkweli.

ذِكْرُ رَحْمَتِ رَبِّكَ عَبْدَهٗ زَكَرِيَّا ③

3. Ukumbusho wa rehema ya Mola wako kwa Mtumishi Wake Zakaria

اِذْ نَادٰى رَبَّهٗ نِدَآءً خَفِيًّا ④

4. Alipomwita Mola wake kwa mwito wa siri.

قَالَ رَبِّ اِنِّيْ وَهَنَ الْعَظْمُ مِنِّيْ وَاشْتَعَلَ الرَّاْسُ شَيْبًا وَّلَمْ اَكُنْۢ بِدُعَآئِكَ رَبِّ شَقِيًّا ⑤

5. Akasema: Mola wangu, bila shaka mfupa wangu umekuwa dhaifu na kichwa kinang'aa kwa mvi wala sikuwa mwenye bahati mbaya, Mola wangu, kwa kukuomba.

Sura hii imepewa jina la mama wa Nabii Isa, Mariamu, kwa maana habari zake za kumzaa Nabii Isa zimeelezwa ndani yake. Ni wazi kuwa sehemu inayoeleza kuzaliwa kwa Nabii Isa ilishuka mapema katika Makka yumkini katika mwaka wa tano baada ya Mtume kupewa utume.

Aya 2. *Kaaf Haa Yaa 'Ain Saad.* Hizi ni herufi za mkato za sifa za Allah *Kaaf* ni *Kariim* (Mkarimu), *Haa* ni *Haadi* (Mwongozi), *Yaa* ni *Ya'jiru walaa yu'jaru 'alaihi* (Anayewapa watu himaya Yake lakini hakuna awezaye kupata himaya kinyume Chake), *'Ain* ni *'Aliim* (Mjuzi wa kila kitu), *Saad* ni *Swaadiqul-wa'd* (mkweli wa ahadi). Maneno hayo yanaonyesha ya kuwa madhumuni ya sura Maryam yatathibitisha kuwa Allah ni Mkarimu, Mwongozi, Kwake ni makimbilio ya wanyonge, Yu Mjuzi wa kila kitu na Mkweli wa ahadi.

Aya 5. *Mola wangu bila shaka mfupa wangu umekuwa dhaifu.* (a) Nabii Zakaria alikuwa na umri zaidi kuliko miaka sabini alipoomba kwa Mungu apate mtoto. (b) Aliomba kwa unyenyekevu sana, na wakati wa kuomba anakiri kwa njia ya ajabu, kuwa yeye hawezi kupata mtoto ila kwa rehema ya Mungu tu, au sivyo haiwezekani mwanamke tasa aliye na mume mzee apate kuzaa. (c) Allah ameeleza habari za kuzaliwa Yahya kabla ya kueleza habari za kuzaliwa Yesu ili kuwatanabahisha Wakristo na Mayahudi. Mayahudi wamehadharishwa kuwa sasa wakati umekaribia kwisha, na ya kwamba wameharibika mno na kwa ajili hii Mungu amemchagua mwanamke tasa na mwanamume mzee kwa ajili ya kumzaa Nabii Wake. Na Wakristo wameambiwa kwamba kuzaliwa kwa Yesu si dalili ya uungu wake ingawa ni namna moja ya ajabu, lakini ajabu ya namna hiyo inapatikana katika kuzaliwa kwa Yahya pia.

6. Na hakika mimi nawahofia jamaa zangu baada yangu, na mke wangu ni tasa, basi Unipe mrithi kutoka Kwako,

وَاِنِّیْ خِفْتُ الْمَوَالِیَ مِنْ وَّرَآءِیْ وَكَانَتِ امْرَاَتِیْ عَاقِرًا فَهَبْ لِیْ مِنْ لَّدُنْكَ وَلِیًّا ۙ﴿۶﴾

7. Atakayenirithi na kuwarithi watu wa Yakubu na Ukamfanye, Mola wangu, aridhishaye.

یَّرِثُنِیْ وَیَرِثُ مِنْ اٰلِ یَعْقُوْبَ ۫ وَاجْعَلْهُ رَبِّ رَضِیًّا ﴿۷﴾

8. Ewe Zakaria, hakika Tunakupa habari njema ya mtoto, jina lake Yahya: Hatujamfanya kabla mwenye jina kama lake·

یٰزَكَرِیَّاۤ اِنَّا نُبَشِّرُكَ بِغُلٰمِ ِۨاسْمُهٗ یَحْیٰی ۙ لَمْ نَجْعَلْ لَّهٗ مِنْ قَبْلُ سَمِیًّا ﴿۸﴾

9. Akasema: Mola wangu! nitapataje mtoto hali mke wangu ni tasa, na mimi nimekwisha fikia uzee wa kupita kiasi.

قَالَ رَبِّ اَنّٰی یَكُوْنُ لِیْ غُلٰمٌ وَّكَانَتِ امْرَاَتِیْ عَاقِرًا وَّقَدْ بَلَغْتُ مِنَ الْكِبَرِ عِتِیًّا ﴿۹﴾

10. Akasema, Ni kama hivyo, Amesema Mola wako: Haya ni rahisi Kwangu, na kwa yakini Nilikuumba zamani nawe hukuwa cho chote.

قَالَ كَذٰلِكَ ۚ قَالَ رَبُّكَ هُوَ عَلَیَّ هَیِّنٌ وَّقَدْ خَلَقْتُكَ مِنْ قَبْلُ وَلَمْ تَكُ شَیْـًٔا ﴿۱۰﴾

11. Akasema: Mola wangu, Unifanyie Ishara. Akasema: Ishara yako ni kuwa hutasema na watu kwa siku tatu kamili.

قَالَ رَبِّ اجْعَلْ لِّیْۤ اٰیَةً ؕ قَالَ اٰیَتُكَ اَلَّا تُكَلِّمَ النَّاسَ ثَلٰثَ لَیَالٍ سَوِیًّا ﴿۱۱﴾

Aya 6. *Mimi nawahofia jamaa zangu.* Maneno haya yanaonyesha utukufu wa fikira za Nabii wa Mungu. Nabii Zakaria hataki mtoto ili apate raha katika uzee wake, bali analilia jambo jingine. Anasema, Mola wangu, mimi naogopa ya kuwa watu wabaya wamezidi na watu wema hawaonekani, basi nataka nipate mtoto atakayetukuza jina Lako baada ya kifo changu.

Aya 8. *Tunakupa habari njema ya mtoto*. Neno *Ghulaam* (mtoto) maana yake ni "kijana mpevu." Basi katika maneno haya Nabii Zakaria ameambiwa mtoto atakayepevuka katika uhai wake, na hivyo furaha yake itazidi.

Aya 9. *Nitapataje mtoto.* Isifikiriwe kuwa alikata tamaa, maana Allah amekwisha sema ya kuwa hawakati tamaa katika rehema ya Mungu isipokuwa watu makafiri.

Jambo hasa ni hili ya kuwa Nabii Zakaria alitaka habari hizi zienee sana, watu wapate kujua jinsi Allah alivyo Mrehemevu; ndiyo maana akauliza maswali na kutaka awekewe alama.

Aya 11. *Hutasema na watu.* Nabii Zakaria alitaka awekewe alama fulani ili watu wengi waweze kupata habari. Mungu anamwekea alama moja akisema, Usiseme na watu siku tatu kamili, bali umtukuze Mungu na uombe tu. Nabii Zakaria alifuata Maagizo ya Mungu, na kwa njia hii wakapatikana mashahidi wengi wa Ishara hiyo, na ikathibitika kuwa Allah ni mkarimu, Mwongozi, Mjuzi wa kila kitu na Mkweli wa ahadi.

Matabibu husema kuwa "unyamavu" ni dawa kubwa ya kutia nguvu katika viungo ili mtu apate kuzaa.

فَخَرَجَ عَلٰى قَوْمِهٖ مِنَ الْمِحْرَابِ فَاَوْحٰۤى اِلَيْهِمْ اَنْ سَبِّحُوْا بُكْرَةً وَّعَشِيًّا ﴿١٢﴾

12. Basi akawatokea watu wake kutoka mihirabuni na akawaashiria ya kwamba: Mtukuzeni (Allah) asubuhi na jioni.

يٰيَحْيٰى خُذِ الْكِتٰبَ بِقُوَّةٍ ؕ وَاٰتَيْنٰهُ الْحُكْمَ صَبِيًّا ۙ﴿١٣﴾

13. Ewe Yahya: Shika Kitabu kwa nguvu; na Tukampa hekima angali mtoto,

وَّحَنَانًا مِّنْ لَّدُنَّا وَزَكٰوةً ؕ وَكَانَ تَقِيًّا ۙ﴿١٤﴾

14. Na huruma kutoka Kwetu, na utakaso, naye alikuwa mtawa.

وَّبَرًّا بِوَالِدَيْهِ وَلَمْ يَكُنْ جَبَّارًا عَصِيًّا ﴿١٥﴾

15. Na mwema kwa wazazi wake, wala hakuwa jeuri, asi.

وَالسَّلٰمُ عَلَيْهِ يَوْمَ وُلِدَ وَيَوْمَ يَمُوْتُ وَيَوْمَ يُبْعَثُ حَيًّا ﴿١٦﴾

16. Na amani iko juu yake siku ali-yozaliwa na siku atakayofariki, na siku atakayofufuliwa hai.

FUNGU 2

وَاذْكُرْ فِى الْكِتٰبِ مَرْيَمَ ۘ اِذِ انْتَبَذَتْ مِنْ اَهْلِهَا مَكَانًا شَرْقِيًّا ۙ﴿١٧﴾

17. Na umtaje Mariamu Kitabuni alipojitenga na jamaa zake, (akaenda) mahali upande wa mashariki.

فَاتَّخَذَتْ مِنْ دُوْنِهِمْ حِجَابًا ۖ فَاَرْسَلْنَاۤ اِلَيْهَا رُوْحَنَا فَتَمَثَّلَ لَهَا بَشَرًا سَوِيًّا ﴿١٨﴾

18. Na akaweka pazia kujikinga nao; kisha Tukampelekea Malaika Wetu ali-yejimithilisha kwake (kama) mtu kamili.

قَالَتْ اِنِّىْۤ اَعُوْذُ بِالرَّحْمٰنِ مِنْكَ اِنْ كُنْتَ تَقِيًّا ﴿١٩﴾

19. (Mariamu) akasema: Hakika mimi najikinga kwa mwingi wa rehema Aniepushe nawe, ikiwa umetakasika.

قَالَ اِنَّمَاۤ اَنَا رَسُوْلُ رَبِّكِ ۖ لِاَهَبَ لَكِ غُلٰمًا زَكِيًّا ﴿٢٠﴾

20. (Malaika) akasema: Hakika mimi ni Mjumbe wa Mola wako; ili nikupe mwana mtakatifu.

Aya 13. *Shika Kitabu kwa nguvu,* yaani Taurati.

Tukampa hekima angali mtoto. Yahya hata katika utoto wake alikuwa mtu mwenye akili na busara.

Aya 17. Baada ya kueleza habari za Yahya Mungu anaeleza habari za Mariamu, mama wa Nabii Isa, ya kuwa alipobalehe alijitenga na watu aliokuwa akikaa nao katika hekalu, na akakaa peke yake mpaka Malaika wa Mungu, Jibrili, alipomtokea katika sura ya mtu na akampasha habari ya kuzaliwa Nabii Isa.

قَالَتْ اَنّٰى يَكُوْنُ لِيْ غُلٰمٌ وَّلَمْ يَمْسَسْنِيْ
بَشَرٌ وَّلَمْ اَكُ بَغِيًّا ﴿٢١﴾

21. Akasema: Ninawezaje kupata mtoto hali hajanigusa mwanamume ye yote wala mimi si asherati?

قَالَ كَذٰلِكِ ۚ قَالَ رَبُّكِ هُوَ عَلَيَّ هَيِّنٌ ۚ
وَلِنَجْعَلَهٗۤ اٰيَةً لِّلنَّاسِ وَ رَحْمَةً مِّنَّا ۚ
وَكَانَ اَمْرًا مَّقْضِيًّا ﴿٢١﴾

22. (Malaika) akasema: Ni kama hivyo; Mola wako Amesema: Haya ni rahisi Kwangu, na ili Tumfanye Ishara kwa wanadamu na rehema itokayo Kwetu; na ni jambo limekwisha hukumiwa.

فَحَمَلَتْهُ فَانْتَبَذَتْ بِهٖ مَكَانًا قَصِيًّا ﴿٢٢﴾

23. Basi akabeba mimba yake, na akaondoka nayo mpaka mahali pa mbali.

فَاَجَآءَهَا الْمَخَاضُ اِلٰى جِذْعِ النَّخْلَةِ ۚ
قَالَتْ يٰلَيْتَنِيْ مِتُّ قَبْلَ هٰذَا وَ كُنْتُ
نَسْيًا مَّنْسِيًّا ﴿٢٤﴾

24. Kisha uchungu ukampeleka penye shina la mtende, akasema: Laiti ningekufa kabla ya haya, na ningekuwa sahau iliyosahauliwa.

فَنَادٰىهَا مِنْ تَحْتِهَاۤ اَلَّا تَحْزَنِيْ قَدْ جَعَلَ
رَبُّكِ تَحْتَكِ سَرِيًّا ﴿٢٥﴾

25. Mara ikamfikia sauti kutoka chini yake: Usihuzunike, hakika Mola wako Ameweka kijito chini yako;

وَهُزِّيْۤ اِلَيْكِ بِجِذْعِ النَّخْلَةِ تُسٰقِطْ
عَلَيْكِ رُطَبًا جَنِيًّا ﴿٢٦﴾

26. Na ulitikise kwako shina la mtende, litakuangushia tende nzuri, zilizo mbivu.

فَكُلِيْ وَاشْرَبِيْ وَقَرِّيْ عَيْنًا ۚ فَاِمَّا تَرَيِنَّ
مِنَ الْبَشَرِ اَحَدًا ۙ فَقُوْلِيْۤ اِنِّيْ نَذَرْتُ
لِلرَّحْمٰنِ صَوْمًا فَلَنْ اُكَلِّمَ الْيَوْمَ
اِنْسِيًّا ۚ ﴿٢٧﴾

27. Basi ule na unywe na uburudishe macho; na kama ukimwona mtu ye yote, useme: Hakika mimi nimeweka nadhiri kwa Mungu wa rehema ya kufunga saumu, kwa hiyo leo sitasema na mtu.

Aya 21. Hakuna shaka Mariamu alizaa mtoto pasipo kushirikiana na mwanamume ye yote. Jambo hili si gumu kwa Mungu. Wakristo wanakubali kuwa Mungu alimwumba Adamu bila baba wala mama, hivyo mbele ya jambo hili si ajabu kitu kama Yesu alizaliwa bila baba.

Aya 24. *Uchungu ukampeleka penye shina la mtende.* Mungu anataka kuwaonyesha Wakristo kuwa Yesu alizaliwa na mwanamke mmoja aliyemzaa kwa taabu nyingi, na kwa shida sana; hivyo kumwita Mungu mzaliwa wa namna hii ni dhuluma kubwa.

Aya 25. Malaika wa Mungu anamwambia Mariamu kuwa hapa chini ya kilima pana chemchem ya maji, basi nenda ukayatumie na upate raha.

فَاَتَتْ بِهٖ قَوْمَهَا تَحْمِلُهٗ ؕ قَالُوْا يٰمَرْيَمُ
لَقَدْ جِئْتِ شَيْـًٔا فَرِيًّا ﴿٢٨﴾

28. Kisha akamleta kwa jamaa zake akisafiri naye. Wakasema: Ewe Mariamu, hakika umetenda kitendo kibaya!

يٰۤاُخْتَ هٰرُوْنَ مَا كَانَ اَبُوْكِ امْرَاَ سَوْءٍ
وَّمَا كَانَتْ اُمُّكِ بَغِيًّا ﴿٢٩﴾

29. Ewe dada wa Harun! baba yako hakuwa mtu mbaya wala mama yako hakuwa asherati.

فَاَشَارَتْ اِلَيْهِ ؕ قَالُوْا كَيْفَ نُكَلِّمُ مَنْ
كَانَ فِى الْمَهْدِ صَبِيًّا ﴿٣٠﴾

30. Ndipo akaashiria kwake. Wakasema: Tuzungumzeje na aliyekuwa mtoto kitandani?

قَالَ اِنِّىْ عَبْدُ اللّٰهِ ۖ اٰتٰنِىَ الْكِتٰبَ
وَجَعَلَنِىْ نَبِيًّا ﴿٣١﴾

31. Akasema: Hakika mimi ni Mtumishi wa Allah; Amenipa Kitabu na Amenifanya Nabii.

وَّجَعَلَنِىْ مُبٰرَكًا اَيْنَ مَا كُنْتُ ۪
وَاَوْصٰنِىْ بِالصَّلٰوةِ وَالزَّكٰوةِ مَا دُمْتُ
حَيًّا ﴿٣٢﴾

32. Na Amenifanya mbarikiwa po pote nilipo, na Amenuisia Sala na Zaka maadamu ningali hai;

وَّبَرًّا بِوَالِدَتِىْ ۫ وَلَمْ يَجْعَلْنِىْ جَبَّارًا
شَقِيًّا ﴿٣٣﴾

33. Na kumfanyia mema mama yangu, wala Hakunifanya niwe jeuri, mwenye bahati mbaya.

وَالسَّلٰمُ عَلَىَّ يَوْمَ وُلِدْتُّ وَيَوْمَ اَمُوْتُ
وَيَوْمَ اُبْعَثُ حَيًّا ﴿٣٤﴾

34. Na amani iko juu yangu siku niliyozaliwa na siku nitakayokufa na siku nitakayofufuliwa kuwa hai.

Aya 28. *Kitu kigeni.* Mayahudi wanamkemea Mariamu na wanamwambia kuwa amezaa mtoto pasipo mume, na jambo hili ni la aibu kubwa.

Aya 29. *Ewe dada wa Harun*. Mayahudi wanamlaumu Mariamu na wanamwambia, Wewe ulijitoa katika njia ya Mungu ukidai kuwa mfuasi wa Nabii Harun, basi u wapi sasa utawa wako na ukuhani wako ambao ulirithi kwa Harun? (Tazama Sura Aali 'Imraan).

Aya 30. Mayahudi wanakataa hata kuzungumza na Nabii Isa na wanasema atajuaje habari hizi naye ni mtoto wa juzi juzi.

Aya 31. Ingawa Mayahudi hawataki kuzungumza na Isa, lakini yeye anaanza kuwahubiria, na mahubiri yake yanaondoa madoa yote kwa Mariamu mama yake. Anawaambia kuwa kwa mujibu wa Taurati mwana haramu hawezi kuingia katika ufalme wa Mungu, lakini niangalieni mimi, Mungu amenihurumia, na amenipamba kwa neema zake hata amenifanya niwe Mtumishi Wake. Nimepewa elimu ya Taurati na amenifanya Nabii. Je, mwana haramu anaweza kupata neema za namna hii?

Aya 32. *Ameniusia Sala na Zaka.* Nabii Isa anasema kuwa amelazimishwa kusali na kutoa zaka daima katika uhai wake. Basi kama yu hai mbinguni hata sasa, je, anasali sala gani, ya Kiislamu au sala ya Kinasara? Na zaka zake anampa nani, je wako watu mbinguni wanaopokea zaka zake?

Aya 34. Katika Aya hii Nabii Isa anaeleza nyakati tatu muhimu: (1) siku ya kuzaliwa

ذٰلِكَ عِيْسَى ابْنُ مَرْيَمَ ۚ قَوْلَ الْحَقِّ الَّذِيْ فِيْهِ يَمْتَرُوْنَ ﴿٣٥﴾

35. Huyo ndiye Isa bin Mariamu. Ndiyo kauli ya haki ambayo wanaifanyia shaka.

مَا كَانَ لِلّٰهِ اَنْ يَّتَّخِذَ مِنْ وَّلَدٍ ۙ سُبْحٰنَهٗ ؕ اِذَا قَضٰۤى اَمْرًا فَاِنَّمَا يَقُوْلُ لَهٗ كُنْ فَيَكُوْنُ ﴿٣٦﴾

36. Haimpasi Allah Ajipangie mwana; Ametakasika; Anapolitaka jambo basi huliambia: Kuwa, nalo huwa.

وَ اِنَّ اللّٰهَ رَبِّيْ وَ رَبُّكُمْ فَاعْبُدُوْهُ ؕ هٰذَا صِرَاطٌ مُّسْتَقِيْمٌ ﴿٣٧﴾

37. Na hakika Allah ni Mola wangu na Mola wenu, basi Mwabuduni; hii ni njia iliyonyoka.

فَاخْتَلَفَ الْاَحْزَابُ مِنْۢ بَيْنِهِمْ ۚ فَوَيْلٌ لِّلَّذِيْنَ كَفَرُوْا مِنْ مَّشْهَدِ يَوْمٍ عَظِيْمٍ ﴿٣٨﴾

38. Lakini makundi yakahitilafiana wao kwa wao. Basi ole kwa wale waliokufuru kwa kuhudhuria Siku iliyo kuu.

اَسْمِعْ بِهِمْ وَاَبْصِرْ ۙ يَوْمَ يَاْتُوْنَنَا لٰكِنِ الظّٰلِمُوْنَ الْيَوْمَ فِيْ ضَلٰلٍ مُّبِيْنٍ ﴿٣٩﴾

39. Watasikia na wataona vizuri vilioje Siku watakayotufikia; lakini wadhalimu siku hiyo watakuwa katika maangamio dhahiri.

وَاَنْذِرْهُمْ يَوْمَ الْحَسْرَةِ اِذْ قُضِيَ الْاَمْرُ ۘ وَهُمْ فِيْ غَفْلَةٍ وَّ هُمْ لَا يُؤْمِنُوْنَ ﴿٤٠﴾

40. Na uwaonye siku ya majuto shauri litakapokatwa; nao wamo katika usahaulifu wala hawaamini.

اِنَّا نَحْنُ نَرِثُ الْاَرْضَ وَمَنْ عَلَيْهَا وَاِلَيْنَا يُرْجَعُوْنَ ﴿٤١﴾ ع ٢

41. Bila shaka Sisi Tutairithi ardhi na walioko juu yake, na Kwetu watarejeshwa.

FUNGU 3

وَاذْكُرْ فِي الْكِتٰبِ اِبْرٰهِيْمَ ۘ اِنَّهٗ كَانَ صِدِّيْقًا نَّبِيًّا ﴿٤٢﴾

42. Na umkumbuke Ibrahimu katika Kitabu, bila shaka yeye alikuwa mkweli sana, Nabii.

kwake; (2) siku ya kufa kwake; (3) siku ya kufufuka kwake. Imekuwaje hataji siku za kukaa kwake mbinguni nazo hazipungui kuliko miaka elfu mbili? Ndugu zetu Waislamu wasiwasaidie Wakristo bure kudhani kuwa Yesu yuko hai mbinguni mpaka sasa pamoja na mwili wake. Bali wajue ya kuwa Nabii Isa amekwisha kufa kama vile walivyokufa Mitume wote wa kabla yake na baada yake.

Aya 42. Katika baadhi ya Hadithi imeelezwa ya kuwa Nabii Ibrahimu alisema uwongo mara tatu. Lakini Aya hii ya Qur'an inaonyesha kwamba Hadithi hiyo si sahihi, na inasema kuwa Nabii Ibrahimu alikuwa mkweli sana. Kanuni inayotakiwa kukumbukwa ni hii ya kwamba kila Hadithi inayopingana na Qur'an si sahihi.

43. Alipomwambia baba yake: Ee baba yangu, kwa nini unamwabudu asiyesikia na asiyeona wala asiyekufaa cho chote?

اِذْ قَالَ لِاَبِيْهِ يٰٓاَبَتِ لِمَ تَعْبُدُ مَا لَا يَسْمَعُ وَلَا يُبْصِرُ وَلَا يُغْنِيْ عَنْكَ شَيْـًٔا ﴿٤٢﴾

44. Ewe baba yangu! kwa yakini imenifikia elimu isiyokufikia, basi nifuate nitakuongoza njia iliyo sawa.

يٰٓاَبَتِ اِنِّيْ قَدْ جَآءَنِيْ مِنَ الْعِلْمِ مَا لَمْ يَاْتِكَ فَاتَّبِعْنِيْٓ اَهْدِكَ صِرَاطًا سَوِيًّا ﴿٤٣﴾

45. Ee baba yangu! usimwabudu Shetani, hakika Shetani ni mwasi kwa Rahmani,

يٰٓاَبَتِ لَا تَعْبُدِ الشَّيْطٰنَ ؕ اِنَّ الشَّيْطٰنَ كَانَ لِلرَّحْمٰنِ عَصِيًّا ﴿٤٤﴾

46. Ewe baba yangu! hakika mimi naogopa ya kwamba itakugusa adhabu kutoka kwa Rahmani, hivyo utakuwa rafiki wa Shetani.

يٰٓاَبَتِ اِنِّيْٓ اَخَافُ اَنْ يَّمَسَّكَ عَذَابٌ مِّنَ الرَّحْمٰنِ فَتَكُوْنَ لِلشَّيْطٰنِ وَلِيًّا ﴿٤٥﴾

47. Akasema: Je unaichukia miungu yangu, ewe Ibrahimu? Kama huachi lazima nitakupiga mawe na uniondokelee mbali kwa muda mchache.

قَالَ اَرَاغِبٌ اَنْتَ عَنْ اٰلِهَتِيْ يٰٓاِبْرٰهِيْمُ ۚ لَئِنْ لَّمْ تَنْتَهِ لَاَرْجُمَنَّكَ وَاهْجُرْنِيْ مَلِيًّا ﴿٤٦﴾

48. (Ibrahimu) akasema: Amani iwe juu yako, nitakuombea msamaha kwa Mola wangu, bila shaka Yeye Ananihurumia sana.

قَالَ سَلٰمٌ عَلَيْكَ ۚ سَاَسْتَغْفِرُ لَكَ رَبِّيْ ؕ اِنَّهٗ كَانَ بِيْ حَفِيًّا ﴿٤٧﴾

49. Nami ninawaondokeeni na mnayoyaabudu kinyume cha Allah, na nitamwomba Mola wangu: huenda sitakuwa na mkosi kwa kumwomba Mola wangu.

وَاَعْتَزِلُكُمْ وَمَا تَدْعُوْنَ مِنْ دُوْنِ اللّٰهِ وَاَدْعُوْا رَبِّيْ ۖ عَسٰٓى اَلَّآ اَكُوْنَ بِدُعَآءِ رَبِّيْ شَقِيًّا ﴿٤٨﴾

50. Basi alipojitenga nao na wanayoyaabudu kinyume cha Allah, Tukampa Isihaka na Yakubu; na kila mmoja Tukamfanya Nabii.

فَلَمَّا اعْتَزَلَهُمْ وَمَا يَعْبُدُوْنَ مِنْ دُوْنِ اللّٰهِ ۙ وَهَبْنَا لَهٗٓ اِسْحٰقَ وَيَعْقُوْبَ ؕ وَكُلًّا جَعَلْنَا نَبِيًّا ﴿٤٩﴾

51. Na Tukawapa katika rehema Zetu, na Tukawafanyia sifa za kweli zilizo kuu.

وَوَهَبْنَا لَهُمْ مِّنْ رَّحْمَتِنَا وَجَعَلْنَا لَهُمْ لِسَانَ صِدْقٍ عَلِيًّا ﴿٥٠﴾ ع

Aya 46. *Ewe baba yangu.* Hakuwa baba yake mzazi, bali baba yake mdogo aitwaye Azar.

Aya 49. *Nami nawaondokeeni.* Alijitenga nao na akahamia nchi ya Sham.

FUNGU 4

وَاذْكُرْ فِي الْكِتٰبِ مُوْسٰٓى ۫ اِنَّهٗ كَانَ مُخْلَصًا وَّكَانَ رَسُوْلًا نَّبِيًّا ﴿٥٢﴾

52. Na umkumbuke Musa katika Kitabu, hakika yeye alikuwa mteule, na alikuwa Mtume, Nabii.

وَنَادَيْنٰهُ مِنْ جَانِبِ الطُّوْرِ الْاَيْمَنِ وَقَرَّبْنٰهُ نَجِيًّا ﴿٥٣﴾

53. Na Tukamwita upande wa kuume wa mlima na Tukamsogeza kuzungumza naye kwa siri.

وَوَهَبْنَا لَهٗ مِنْ رَّحْمَتِنَآ اَخَاهُ هٰرُوْنَ نَبِيًّا ﴿٥٤﴾

54. Nasi Tukampa, katika rehema Zetu, nduguye Harun, Nabii.

وَاذْكُرْ فِي الْكِتٰبِ اِسْمٰعِيْلَ ۫ اِنَّهٗ كَانَ صَادِقَ الْوَعْدِ وَكَانَ رَسُوْلًا نَّبِيًّا ﴿٥٥﴾ ۚ

55. Na umkumbuke katika Kitabu Ismaili, bila shaka yeye alikuwa mkweli wa ahadi, na alikuwa Mtume, Nabii.

وَكَانَ يَاْمُرُ اَهْلَهٗ بِالصَّلٰوةِ وَالزَّكٰوةِ ۖ وَكَانَ عِنْدَ رَبِّهٖ مَرْضِيًّا ﴿٥٦﴾

56. Na alikuwa akiwaamuru watu wake Sala na Zaka na alikuwa mridhiwa mbele ya Mola wake.

وَاذْكُرْ فِي الْكِتٰبِ اِدْرِيْسَ ۫ اِنَّهٗ كَانَ صِدِّيْقًا نَّبِيًّا ﴿٥٧﴾ ۙ

57. Na umkumbuke Idrisa katika Kitabu, bila shaka yeye alikuwa mkweli sana, Nabii,

وَّرَفَعْنٰهُ مَكَانًا عَلِيًّا ﴿٥٨﴾

58. Na Tulimnyanyua daraja ya juu.

اُولٰٓئِكَ الَّذِيْنَ اَنْعَمَ اللّٰهُ عَلَيْهِمْ مِّنَ النَّبِيّٖنَ مِنْ ذُرِّيَّةِ اٰدَمَ ۗ وَمِمَّنْ حَمَلْنَا مَعَ نُوْحٍ ۖ وَّمِنْ ذُرِّيَّةِ اِبْرٰهِيْمَ وَاِسْرَآءِيْلَ ۖ وَمِمَّنْ هَدَيْنَا وَاجْتَبَيْنَا ؕ اِذَا تُتْلٰى عَلَيْهِمْ اٰيٰتُ الرَّحْمٰنِ خَرُّوْا سُجَّدًا وَّبُكِيًّا ﴿٥٩﴾ ۩

59. Hao ndio Aliowaneemesha Allah, miongoni mwa Manabii, katika wazao wa Adamu, na katika wale Tuliowapandisha pamoja na Nuhu, na katika wazao wa Ibrahimu na Israeli, na katika wale Tuliowaongoza na Tukawachagua; wanaposomewa Aya za Rahmani huanguka kusujudu na kulia.

فَخَلَفَ مِنْۢ بَعْدِهِمْ خَلْفٌ اَضَاعُوا الصَّلٰوةَ وَاتَّبَعُوا الشَّهَوٰتِ فَسَوْفَ يَلْقَوْنَ غَيًّا ﴿٦٠﴾ ۙ

60. Lakini wakaandamia baada yao wazao wabaya, wakaharibu Sala na wakafuata matamanio mabaya; kwa hiyo hivi karibuni watakuta maangamizo,

Aya 52. *Rasuulan-Nabiyya.* "Mtume, Nabii." Neno *Rasuul* maana yake ni "aliyetumwa" na *Nabii* maana yake ni "mwenye kutoa habari." Basi kila Mtume ni Nabii na kila Nabii ni Mtume. Watu wengine wanasema *Rasuul* anakuwa mwenye Kitabu, na *Nabii* haji na Kitabu kipya; lakini tafsiri hii haipatani na Qur'an. Kwa mfano; katika Aya 55 Ismail ameitwa *Rasuul* na *Nabii* pia.

61. Isipokuwa anayetubu na kuamini na kufanya yaliyo mema, basi hao wataingia Peponi wala hawatadhulumiwa cho chote:

إِلَّا مَنْ تَابَ وَاٰمَنَ وَعَمِلَ صَالِحًا فَاُولٰٓئِكَ يَدْخُلُوْنَ الْجَنَّةَ وَلَا يُظْلَمُوْنَ شَيْـًٔا ﴿٦١﴾

62. Pepo za milele ambazo Mungu wa rehema Amewaahidi watumishi Wake zilizo katika siri; bila shaka ahadi Yake ni yenye kufika.

جَنّٰتِ عَدْنِ ِالَّتِيْ وَعَدَ الرَّحْمٰنُ عِبَادَهٗ بِالْغَيْبِ ؕ اِنَّهٗ كَانَ وَعْدُهٗ مَاْتِيًّا ﴿٦٢﴾

63. Hawatasikia humo upuuzi ila, Amani; na watapata humo riziki zao asubuhi na jioni.

لَا يَسْمَعُوْنَ فِيْهَا لَغْوًا اِلَّا سَلٰمًا ؕ وَلَهُمْ رِزْقُهُمْ فِيْهَا بُكْرَةً وَّعَشِيًّا ﴿٦٣﴾

64. Hiyo ndiyo Pepo Tutakayomrithisha katika watumishi Wetu ambaye ni mchaji.

تِلْكَ الْجَنَّةُ الَّتِيْ نُوْرِثُ مِنْ عِبَادِنَا مَنْ كَانَ تَقِيًّا ﴿٦٤﴾

65. Wala hatuteremki ila kwa amri ya Mola wako. Anayo yaliyoko mbele yetu na yaliyoko nyuma yetu na yaliyomo katikati ya hayo; na Mola wako si mwenye kusahau.

وَمَا نَتَنَزَّلُ اِلَّا بِاَمْرِ رَبِّكَ ۚ لَهٗ مَا بَيْنَ اَيْدِيْنَا وَمَا خَلْفَنَا وَمَا بَيْنَ ذٰلِكَ ۚ وَمَا كَانَ رَبُّكَ نَسِيًّا ﴿٦٥﴾

66. Mola wa mbingu na ardhi na vilivyomo kati yao, basi umwabudu na udumu katika ibada Yake. Je, unamjua (mwingine) mwenye jina kama Lake?

رَبُّ السَّمٰوٰتِ وَالْاَرْضِ وَمَا بَيْنَهُمَا فَاعْبُدْهُ وَاصْطَبِرْ لِعِبَادَتِهٖ ؕ هَلْ تَعْلَمُ لَهٗ سَمِيًّا ﴿٦٦﴾ ع ٧

FUNGU 5

67. Na mwanadamu husema: Je, nitakapokuwa nimekufa, kweli nitafufuliwa kuwa hai?

وَيَقُوْلُ الْاِنْسَانُ ءَاِذَا مَا مِتُّ لَسَوْفَ اُخْرَجُ حَيًّا ﴿٦٧﴾

68. Je, mwanadamu hakumbuki ya kwamba Tulimwumba kabla hali hakuwa cho chote?

اَوَلَا يَذْكُرُ الْاِنْسَانُ اَنَّا خَلَقْنٰهُ مِنْ قَبْلُ وَلَمْ يَكُ شَيْـًٔا ﴿٦٨﴾

69. Basi kwa kiapo cha Mola wako kwa yakini Tutawakusanya wao pamoja na mashetani; kisha bila shaka Tutawahudhurisha pembezoni mwa Jahanamu, wakiangukia magoti.

فَوَرَبِّكَ لَنَحْشُرَنَّهُمْ وَالشَّيٰطِيْنَ ثُمَّ لَنُحْضِرَنَّهُمْ حَوْلَ جَهَنَّمَ جِثِيًّا ﴿٦٩﴾ ع

70. Kisha kwa yakini Tutawatoa katika kila taifa wale miongoni mwao waliomwasi zaidi Mungu wa huruma.

ثُمَّ لَنَنْزِعَنَّ مِنْ كُلِّ شِيْعَةٍ اَيُّهُمْ اَشَدُّ عَلَى الرَّحْمٰنِ عِتِيًّا ﴿٧٠﴾ ع

71. Tena hakika Sisi Tunawafahamu sana wanaostahili zaidi kuunguzwa humo.

ثُمَّ لَنَحْنُ اَعْلَمُ بِالَّذِيْنَ هُمْ اَوْلٰى بِهَا صِلِيًّا ﴿٧١﴾

72. Wala hakuna ye yote katika ninyi ila ni mwenye kuifikia. Ndiyo wajibu juu ya Mola wako uliokwisha hukumiwa.

وَاِنْ مِّنْكُمْ اِلَّا وَارِدُهَا ۚ كَانَ عَلٰى رَبِّكَ حَتْمًا مَّقْضِيًّا ﴿٧٢﴾

73. Kisha Tutawaokoa wale wamchao (Mungu); na Tutawaacha wadhalimu humo wakiangukia magoti.

ثُمَّ نُنَجِّي الَّذِيْنَ اتَّقَوْا وَّنَذَرُ الظّٰلِمِيْنَ فِيْهَا جِثِيًّا ﴿٧٣﴾

74. Na wanaposomewa Aya Zetu zilizo wazi, husema wale walioukufuru kuwaambia walioamini: Lipi katika makundi mawili lina kao jema na lililo bora katika mkutano?

وَاِذَا تُتْلٰى عَلَيْهِمْ اٰيٰتُنَا بَيِّنٰتٍ قَالَ الَّذِيْنَ كَفَرُوْا لِلَّذِيْنَ اٰمَنُوْٓا ۙ اَيُّ الْفَرِيْقَيْنِ خَيْرٌ مَّقَامًا وَّاَحْسَنُ نَدِيًّا ﴿٧٤﴾

75. Na vingapi Tumeviangamiza kabla yao katika vizazi vilivyokuwa na vifaa vizuri mno na virembo zaidi.

وَكَمْ اَهْلَكْنَا قَبْلَهُمْ مِّنْ قَرْنٍ هُمْ اَحْسَنُ اَثَاثًا وَّرِءْيًا ﴿٧٥﴾

76. Sema: Aliye katika upotevu, basi Mungu Mwenye huruma bila shaka Atamzidishia muda mpaka wayaone waliyoonywa - ikiwa ni adhabu au ikiwa ni saa ile - ndipo watajua ni nani mwenye kao baya na aliye dhaifu kwa jeshi.

قُلْ مَنْ كَانَ فِى الضَّلٰلَةِ فَلْيَمْدُدْ لَهُ الرَّحْمٰنُ مَدًّا ۚ حَتّٰٓى اِذَا رَاَوْا مَا يُوْعَدُوْنَ اِمَّا الْعَذَابَ وَاِمَّا السَّاعَةَ ؕ فَسَيَعْلَمُوْنَ مَنْ هُوَ شَرٌّ مَّكَانًا وَّاَضْعَفُ جُنْدًا ﴿٧٦﴾

Aya 72 - 73. *Wala hakuna ye yote katika ninyi ila ni mwenye kuifikia* (Jahanamu), *na kisha Tutawaokoa wale wamachao (Mungu).* Aya hizi zinaonyesha kwamba kila mtu ataingia Motoni na kisha Allah atawalinda watu wema wasipate adhabu. Ndiyo kusema, wataingia Jahanamu pia na watakaa salama pia. Hii haina maana ila maana ya kwamba watu wema watageuza kila kitu kuwa njia ya kuleta starehe kwao kwa ajili ya uzima wa fahamu zao. Mtume *s.a.w.* alisema, "Allah atamwabia mtu: Rukia ndani ya Jahanamu. Atakaporukia ndani yake, ataiona ni mahali papendezapo kabisa."

Akiandika juu ya Aya hii, Seyidna Ahmad *(alaihissalaam)* amesema, "Ni njia yenye taabu namna gani iliyo njia ya Allah. Lakini njia hii hufanywa nyepesi kwa wale wanaojitupa katika shimo la taabu kwa nia ya kufa. Hao wanaohukumu katika mioyo yao kuwa tunakubali moto na tutaungua kwa ajili ya Mpenzi wetu, Allah.' Kisha wao hujitumbukiza katika moto, kumbe moto ule ni Pepo. Na hivi ndivyo alivyosema Allah katika Qur'an: *Wala hakuna ye yote katika ninyi ila ni mwenye kuifikia.* Yaani, enyi watu wabaya na wazuri, hapana ye yote katika ninyi asiyepita kwenye moto wa Jahanamu. Lakini hao wanaounguzwa kwa ajili ya Allah, wataokolewa katika moto. Bali yule mwenye kuunguzwa kwa ajili ya nafsi yake yenye kumwamrisha kutenda mabaya, basi moto utamwunguza. Amebarikiwa yule mwenye kupigana na nafsi yake kwa ajili ya Allah; na bahati mbaya kwa yule anayepigana na Mungu kwa ajili ya nafsi yake" (Safina ya Nuhu).

77. Na Allah Huwazidishia walioongoka mwongozo; na vitendo vizuri vibakiavyo ni bora katika malipo mbele ya Mola wako na bora katika matokeo.

وَيَزِيْدُ اللّٰهُ الَّذِيْنَ اهْتَدَوْا هُدًى ؕ وَالْبٰقِيٰتُ الصّٰلِحٰتُ خَيْرٌ عِنْدَ رَبِّكَ ثَوَابًا وَّخَيْرٌ مَّرَدًّا ﴿٧٦﴾

78. Je, umemwona yule aliyezikataa Aya Zetu na akasema: Kwa hakika nitapewa mali na watoto.

اَفَرَءَيْتَ الَّذِيْ كَفَرَ بِاٰيٰتِنَا وَقَالَ لَاُوْتَيَنَّ مَالًا وَّوَلَدًا ﴿٧٧﴾

79. Je! Amepata habari za ghaibu au amechukua ahadi kwa Mungu wa huruma.

اَطَّلَعَ الْغَيْبَ اَمِ اتَّخَذَ عِنْدَ الرَّحْمٰنِ عَهْدًا ﴿٧٨﴾

80. Siyo! hakika Tutayaandika anayoyasema, na Tutamzidishia muda katika adhabu.

كَلَّا ؕ سَنَكْتُبُ مَا يَقُوْلُ وَنَمُدُّ لَهٗ مِنَ الْعَذَابِ مَدًّا ﴿٧٩﴾

81. Na Tutamrithi anayoyasema na atatufikia peke yake!

وَّنَرِثُهٗ مَا يَقُوْلُ وَيَاْتِيْنَا فَرْدًا ﴿٨٠﴾

82. Na walishika waungu badala ya Allah ili wawe nguvu kwao.

وَاتَّخَذُوْا مِنْ دُوْنِ اللّٰهِ اٰلِهَةً لِّيَكُوْنُوْا لَهُمْ عِزًّا ﴿٨١﴾

83. Wapi! Hivi karibuni watakataa ibada yao na watakuwa mahasimu zao.

كَلَّا ؕ سَيَكْفُرُوْنَ بِعِبَادَتِهِمْ وَيَكُوْنُوْنَ عَلَيْهِمْ ضِدًّا ﴿٨٢﴾ ع ١٧

FUNGU 6

84. Je, huoni ya kwamba Tumewatuma mashetani juu ya makafiri wanaowachochea sana?

اَلَمْ تَرَ اَنَّاۤ اَرْسَلْنَا الشَّيٰطِيْنَ عَلَى الْكٰفِرِيْنَ تَؤُزُّهُمْ اَزًّا ﴿٨٣﴾

85. Basi usiwafanyie haraka maana Tunawahesabia idadi.

فَلَا تَعْجَلْ عَلَيْهِمْ ؕ اِنَّمَا نَعُدُّ لَهُمْ عَدًّا ﴿٨٤﴾

86. Siku Tutakayowakusanya wachaji kuwapeleka kwa Rahman kama wageni.

يَوْمَ نَحْشُرُ الْمُتَّقِيْنَ اِلَى الرَّحْمٰنِ وَفْدًا ﴿٨٥﴾

87. Na Tutawaswaga wakosefu kuelekea kwenye Jahannamu kama kundi la wanyama linavyoswagwa kuelekea mahali pa kunywea maji.

وَّنَسُوْقُ الْمُجْرِمِيْنَ اِلٰى جَهَنَّمَ وِرْدًا ﴿٨٦﴾ ع

88. Hawatakuwa na mamlaka ya kufanya uombezi ila yule aliyeshika ahadi kwa Rahmani.

لَا يَمْلِكُوْنَ الشَّفَاعَةَ اِلَّا مَنِ اتَّخَذَ عِنْدَ الرَّحْمٰنِ عَهْدًا ﴿٨٧﴾ ع

وَقَالُوا اتَّخَذَ الرَّحْمٰنُ وَلَدًا ﴿٨٩﴾

89. Nao husema: Rahmani Amejipangia mwana.

لَقَدْ جِئْتُمْ شَيْـًٔا اِدًّا ﴿٩٠﴾

90. Bila shaka mmeleta jambo lichukizalo.

تَكَادُ السَّمٰوٰتُ يَتَفَطَّرْنَ مِنْهُ وَتَنْشَقُّ الْاَرْضُ وَتَخِرُّ الْجِبَالُ هَدًّا ﴿٩١﴾

91. Karibu mbingu zitatuke kwalo na ardhi ipasuke na milima ianguke vipande-vipande.

اَنْ دَعَوْا لِلرَّحْمٰنِ وَلَدًا ﴿٩٢﴾

92. Kwa sababu wamemdaia Rahmani kuwa na mwana.

وَمَا يَنْۢبَغِيْ لِلرَّحْمٰنِ اَنْ يَّتَّخِذَ وَلَدًا ﴿٩٣﴾

93. Wala haimpasi Rahmani kupanga mwana.

اِنْ كُلُّ مَنْ فِي السَّمٰوٰتِ وَالْاَرْضِ اِلَّآ اٰتِي الرَّحْمٰنِ عَبْدًا ﴿٩٤﴾

94. Hakuna ye yote aliyomo mbinguni na ardhini ila atafika kwa Rahman hali yu mtumishi.

لَقَدْ اَحْصٰىهُمْ وَعَدَّهُمْ عَدًّا ﴿٩٥﴾

95. Kwa yakini Yeye Amekwisha kuwazunguka na Akawahesabu sawasawa.

وَكُلُّهُمْ اٰتِيْهِ يَوْمَ الْقِيٰمَةِ فَرْدًا ﴿٩٦﴾

96. Na kila mmoja wao atamfikia siku ya Kiyama peke yake.

اِنَّ الَّذِيْنَ اٰمَنُوْا وَعَمِلُوا الصّٰلِحٰتِ سَيَجْعَلُ لَهُمُ الرَّحْمٰنُ وُدًّا ﴿٩٧﴾

97. Hakika wale walioamini na kufanya vitendo vizuri lazima Rahmani Atawafanyia upendo.

فَاِنَّمَا يَسَّرْنٰهُ بِلِسَانِكَ لِتُبَشِّرَ بِهِ الْمُتَّقِيْنَ وَتُنْذِرَ بِهٖ قَوْمًا لُّدًّا ﴿٩٨﴾

98. Na hakika Tumeirahisisha (Qur'an) kwa lugha yako ili uwabashirie kwayo wamchao (Mungu) na uwaonye kwayo watu wagombanao.

وَكَمْ اَهْلَكْنَا قَبْلَهُمْ مِّنْ قَرْنٍ ؕ هَلْ تُحِسُّ مِنْهُمْ مِّنْ اَحَدٍ اَوْ تَسْمَعُ لَهُمْ رِكْزًا ﴿٩٩﴾ ع ۱۶ ع

99. Na vingapi Tuliviangamiza kabla yao katika vizazi! Je, unawaona hata mmoja wao au kusikia shindo lao?

سُوْرَةُ طٰهٰ مَكِّيَّةٌ وَّ هِيَ مَعَ الْبَسْمَلَةِ مِائَةٌ وَّ سِتٌّ وَّ ثَلَاثُوْنَ اٰيَةً وَّ ثَمَانِيَةُ رُكُوْعَاتٍ

20. SURA TWAA HAA

Imeteremshwa Makka

Ina mafungu 8 na Aya 136 pamoja na Bismillahi

بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ ①

1. Kwa jina la Allah, Mwingi wa rehema, Mwingi wa ukarimu.

طٰهٰ ②

2. Ewe mtu (kamili)!

مَآ اَنْزَلْنَا عَلَيْكَ الْقُرْاٰنَ لِتَشْقٰٓى ۙ ③

3. Hatukukuteremshia Qur'an ili upate shida.

اِلَّا تَذْكِرَةً لِّمَنْ يَّخْشٰى ۙ ④

4. Bali iwe mawaidha kwa mwenye kunyenyekea.

تَنْزِيْلًا مِّمَّنْ خَلَقَ الْاَرْضَ وَ السَّمٰوٰتِ الْعُلٰى ۚ ⑤

5. Uteremsho kutoka kwa Yule Aliyeumba ardhi na mbingu zilizoinuka.

اَلرَّحْمٰنُ عَلَى الْعَرْشِ اسْتَوٰى ⑥

6. (Ndiye) Mungu wa huruma; Aliyestawi juu ya kiti cha Enzi.

لَهٗ مَا فِي السَّمٰوٰتِ وَ مَا فِي الْاَرْضِ وَ مَا بَيْنَهُمَا وَ مَا تَحْتَ الثَّرٰى ⑦

7. Ni vyake vilivyomo mbinguni na vilivyomo ardhini na vilivyomo kati yao na vilivyomo chini ya udongo.

Jina la sura hii ni herufi zake mbili za mkato za mwanzo.

Yumkini kabisa sura hii ilishuka wakati ule ule wa sura 19. Ibni Hisham na Ibni Sa'd wanaiunganisha sura hii na wakati aliposilimu Seyidna Umar katika mwaka wa sita wa Uislamu, na wanasema ya kuwa sura hii ndiyo iliyosomwa na dada wa Seyidna Umar na ikamtuliza Umar hasira yake na ikamfanya ampende Mtume.

Katika sura hii Allah anaeleza fadhili za Mtume Muhammad *s.a.w.* na jinsi atakavyofanikiwa katika dunia. Kazi ya Manabii wa Mungu ni kusimamisha utukufu na mwongozo katika ulimwengu, na kwa ajili hii Mungu ameleta herufi *Taa Haa* mwanzoni, ili kudhihirisha kuwa yule ambaye mwenyewe ni mtukufu na mwongozi, bila shaka atafanikiwa kusimamisha duniani utukufu na uongozi.

Aya 2. *Taa Haa. Taa* ni *Tayyib* (Mtukufu), *Haa* ni *Haadii* (Mwongozi). Hivyo maneno haya yanafasiriwa "Ewe mtukufu, mwongozi wa watu" yaani Mtume *s.a.w.* Kadhalika neno *Taa Haa* maana yake ni "Ewe Mtu (kamili)" kama tulivyolitafsiri na kama inavyokubaliwa na mufasirina wengi wa mwanzoni kama Ibni Abbas, Katada, Mujahid, Hassan na wengineo.

Aya 3. *Litashqaa,* "Ili upate mashaka." Neno hili pia linaweza kufasiriwa, *ili uwe mwenye bahati mbaya.* Basi hapo Allah anaeleza kuwa haiwezekani kabisa ya kuwa mfuasi wa maneno matukufu kama Qur'an asifanikiwe. Basi Mtume *s.a.w.* na wafuasi wake hawatashindwa, bali watashinda.

8. Na ukinena kwa sauti kubwa, basi hakika Yeye Anajua yaliyo siri na yafichwayo sana.

وَاِنْ تَجْهَرْ بِالْقَوْلِ فَاِنَّهٗ يَعْلَمُ السِّرَّ وَاَخْفَى ۝٨

9. Allah - hakuna aabudiwaye isipokuwa Yeye; Anayo majina mazuri.

اَللّٰهُ لَاۤ اِلٰهَ اِلَّا هُوَ ؕ لَهُ الْاَسْمَآءُ الْحُسْنٰى ۝٩

10. Na je, imekufikia hadithi ya Musa?

وَهَلْ اَتٰىكَ حَدِيْثُ مُوْسٰى ۝١٠

11. Alipouona moto, na akawaambia ahali zake, Ngojeni, hakika nimeona moto, huenda nitawaleteeni kijinga katika huo au nitapata mwongozo kwenye moto.

اِذْ رَاٰ نَارًا فَقَالَ لِاَهْلِهِ امْكُثُوْۤا اِنِّيْۤ اٰنَسْتُ نَارًا لَّعَلِّيْۤ اٰتِيْكُمْ مِّنْهَا بِقَبَسٍ اَوْ اَجِدُ عَلَى النَّارِ هُدًى ۝١١

12. Basi alipoufikia ikanadiwa, Ewe Musa!

فَلَمَّاۤ اَتٰىهَا نُوْدِيَ يٰمُوْسٰى ۝١٢

13. Bila shaka Mimi ndiye Mola wako; basi vua viatu vyako; hakika wewe upo katika bonde Tuwa lililotakasika.

اِنِّيْۤ اَنَا رَبُّكَ فَاخْلَعْ نَعْلَيْكَ ۚ اِنَّكَ بِالْوَادِ الْمُقَدَّسِ طُوًى ۝١٣

14. Nami Nimekuchagua basi uyasikilize yanayofunuliwa.

وَاَنَا اخْتَرْتُكَ فَاسْتَمِعْ لِمَا يُوْحٰى ۝١٤

Aya 8. *Na ukinena kwa sauti kubwa.* Katika Aya hii Allah anasema kwamba kuomba kwa sauti kubwa pia inafaa wakati mwingine, lakini watu wasianze kufikiri ya kuwa hii tu ndiyo njia ya kumsikilizisha Mungu; maana, *Yeye Anajua yaliyo siri na yafichwayo sana. Sirr* ni jambo lililo na mwenye siri ambalo halijulikani kwa watu wengine. *Yafichwayo sana* ni fikira atakazokuwa nazo mtu ambazo yeye mwenyewe hajazijua.

Aya 10. *Imekufikia hadithi ya Musa?* Mtume *s.a.w.* katika wana wa Ismaili ni kama Nabii Musa katika wana wa Israeli. Kwa ajili hii Allah amechagua habari za Nabii Musa kwa kuonyesha kuwa vile kama Musa alivyopata taabu mwanzoni, na mwishoni akafanikiwa, hivyo ndivyo zitakavyokuwa habari za Mtume *s.a.w.*

Aya 11. *Alipouona moto.* Nabii Musa aliona onyesho la kwanza la Allah katika sura ya moto; na moto katika maonyesho ya namna hii unafasiriwa ni vita. Basi Nabii Musa kwa njia ya namna hii akaambiwa, watu wako watashurutishwa kupigana katika njia ya dini. Na hapa Mtume *s.a.w* aliyefanana na Musa anapashwa habari hii hii.

Aya 13. *Vua viatu vyako.* Mtu akiona katika ndoto anaona hali fulani ya viatu vyake, taabiri yake itakuwa ahali zake. Kwa ajili hii masufiya wanasema kuwa hapa Musa ameambiwa kuwa kwa kutaka kupata radhi za Allah inatakiwa kwa muda ajiweke mbali na ahali zake, asishughulike nao, bali ajishughulishe na kumkumbuka Allah.

15. Kwa yakini Mimi ndiye Allah, hakuna aabudiwaye ila Mimi, basi niabudu na usimamishe Sala kwa kunikumbuka.

إِنَّنِيٓ أَنَا ٱللَّهُ لَآ إِلَٰهَ إِلَّآ أَنَا۠ فَٱعۡبُدۡنِي وَأَقِمِ ٱلصَّلَوٰةَ لِذِكۡرِيٓ ١٤

16. Bila shaka saa ile inakuja - karibu Nitaidhihirisha - ili kila nafsi ilipwe kwa yale iliyoyafanyia bidii.

إِنَّ ٱلسَّاعَةَ ءَاتِيَةٌ أَكَادُ أُخۡفِيهَا لِتُجۡزَىٰ كُلُّ نَفۡسِۭ بِمَا تَسۡعَىٰ ١٥

17. Basi asikuzuie katika hayo yule asiyeamini na afuataye matamanio yake, usije ukaangamia.

فَلَا يَصُدَّنَّكَ عَنۡهَا مَن لَّا يُؤۡمِنُ بِهَا وَٱتَّبَعَ هَوَىٰهُ فَتَرۡدَىٰ ١٦

18. Na ni nini kilichomo mkononi mwako wa kuume, ewe Musa?

وَمَا تِلۡكَ بِيَمِينِكَ يَٰمُوسَىٰ ١٧

19. Akasema: Hii ni fimbo yangu, ninaiegemea na ninaiangushia majani kwa mbuzi zangu, tena ninaitumia kwa matumizi mengine.

قَالَ هِيَ عَصَايَ أَتَوَكَّؤُاْ عَلَيۡهَا وَأَهُشُّ بِهَا عَلَىٰ غَنَمِي وَلِيَ فِيهَا مَـَٔارِبُ أُخۡرَىٰ ١٨

20. Akasema: Itupe, ewe Musa.

قَالَ أَلۡقِهَا يَٰمُوسَىٰ ١٩

21. Na akaitupa mara ikawa nyoka anayekimbia.

فَأَلۡقَىٰهَا فَإِذَا هِيَ حَيَّةٞ تَسۡعَىٰ ٢٠

22. Akasema ishike wala usiogope; sasa hivi tutairudisha hali yake ya kwanza.

قَالَ خُذۡهَا وَلَا تَخَفۡۖ سَنُعِيدُهَا سِيرَتَهَا ٱلۡأُولَىٰ ٢١

23. Na bandika mkono wako kwenye kwapa lako utatoka mweupe bila ya kuwa na maradhi: kuwa Ishara nyingine.

وَٱضۡمُمۡ يَدَكَ إِلَىٰ جَنَاحِكَ تَخۡرُجۡ بَيۡضَآءَ مِنۡ غَيۡرِ سُوٓءٍ ءَايَةً أُخۡرَىٰ ٢٢

Aya 21. *Nyoka anayekimbia.* Habari hizi zote ni za *kashfi* (njozi safi). Nabii Musa anaambiwa, watu wake [*asaa* (fimbo), maana yake pia ni kaumu ya watu] wasio na uzima sasa watapewa uzima, na watawauma maadui za Mungu kama aumavyo nyoka, na adui hatakuwa na njia ila kufa. Basi katika *kashfi* hii Nabii Musa anafahamishwa mwanzo wa kazi yake namna ya matokeo yatakayotokea baadaye. Basi hii ni Ishara ya kuwa Mtume *s.a.w.* pia atawahuisha wale waliokuwa hawana uzima kwa karne nyingi, na watapewa uhai kwa mkono wa Mtume *s.a.w.*, na watawashinda maadui wa Mungu.

Aya 23. Ishara ya pili ya Nabii Musa ni mkono mweupe. Ishara hii inaonyesha kuwa kupigana vita si kusudi hasa la Manabii wa Allah, bali kusudi lao hasa ni kusimamisha ukweli katika dunia kwa dalili zilizo wazi. Hivyo Nabii Musa na Nabii Muhammad *s.a.w.* watawashinda maadui zao kwa msaada wa Allah na ushindi wao utang'aa kwa dalili zilizo wazi. Na hivyo ndivyo ilivyotokea. Taurati ilikuwa *mkono mweupe* wa Musa na Qur'an ilikuwa *mkono mweupe* wa Mtume *s.a.w.*

لِنُرِيَكَ مِنْ اٰيٰتِنَا الْكُبْرٰى ﴿٢٤﴾

24. Ili Tukuonyeshe katika Ishara Zetu zilizo kubwa.

اِذْهَبْ اِلٰى فِرْعَوْنَ اِنَّهٗ طَغٰى ﴿٢٥﴾

25. Nenda kwa Firauni bila shaka yeye amepita kiasi.

FUNGU 2

قَالَ رَبِّ اشْرَحْ لِيْ صَدْرِيْ ﴿٢٦﴾

26. Akasema: Mola wangu! Unipanulie kifua changu.

وَيَسِّرْ لِيْٓ اَمْرِيْ ﴿٢٧﴾

27. Na Unifanyie rahisi kazi yangu.

وَاحْلُلْ عُقْدَةً مِّنْ لِّسَانِيْ ﴿٢٨﴾

28. Na ufungue kifungo katika ulimi wangu.

يَفْقَهُوْا قَوْلِيْ ﴿٢٩﴾

29. Wapate kufahamu kauli yangu.

وَاجْعَلْ لِّيْ وَزِيْرًا مِّنْ اَهْلِيْ ﴿٣٠﴾

30. Na unijaalie naibu (msaidizi) katika jamaa zangu -

هٰرُوْنَ اَخِي ﴿٣١﴾

31. Ndugu yangu Harun.

اشْدُدْ بِهٖٓ اَزْرِيْ ﴿٣٢﴾

32. Uniimarishie kwaye nguvu zangu.

وَاَشْرِكْهُ فِيْٓ اَمْرِيْ ﴿٣٣﴾

33. Na Umshirikishe katika kazi yangu,

كَيْ نُسَبِّحَكَ كَثِيْرًا ﴿٣٤﴾

34. Ili tukutukuze sana.

وَّنَذْكُرَكَ كَثِيْرًا ﴿٣٥﴾

35. Na tukutaje kwa wingi.

اِنَّكَ كُنْتَ بِنَا بَصِيْرًا ﴿٣٦﴾

36. Hakika wewe Unatuona.

قَالَ قَدْ اُوْتِيْتَ سُؤْلَكَ يٰمُوْسٰى ﴿٣٧﴾

37. Akasema: Hakika umepewa maombi yako, ewe Musa.

وَلَقَدْ مَنَنَّا عَلَيْكَ مَرَّةً اُخْرٰٓى ﴿٣٨﴾

38. Na hakika Tulikufanyia hisani mara nyingine.

اِذْ اَوْحَيْنَآ اِلٰٓى اُمِّكَ مَا يُوْحٰٓى ﴿٣٩﴾

39. Tulipomfunulia mama yako yanayofunuliwa.

اَنِ اقْذِفِيْهِ فِي التَّابُوْتِ فَاقْذِفِيْهِ فِي الْيَمِّ فَلْيُلْقِهِ الْيَمُّ بِالسَّاحِلِ يَاْخُذْهُ عَدُوٌّ لِّيْ وَعَدُوٌّ لَّهٗ ؕ وَاَلْقَيْتُ عَلَيْكَ مَحَبَّةً مِّنِّيْ ۚ وَلِتُصْنَعَ عَلٰى عَيْنِيْ ﴿٤٠﴾

40. Ya kwamba mtie sandukuni, kisha litie mtoni, na mto utamtupa ufukoni ili amchukue adui Yangu na adui yake. Na Nimekutupia upendo kutoka Kwangu, na ili ulelewe machoni Pangu.

41. (Kumbuka) dada yako alipokwe-nda na akasema: Je, niwajulisheni atakayemlea? Na Tukakurudisha kwa mama yako ili macho yake yaburudike wala asihuzunike. Na ulimwua mtu na Tukakuokoa katika huzuni na Tukakujaribu kwa majaribio. Na ukakaa kwa miaka kadhaa kati ya watu wa Madiani; kisha umefika kama ilivyokadiriwa, ewe Musa.

42. Na Nimekuchagua kwa ajili yangu.

43. Nenda wewe na ndugu yako pamoja na Ishara Zangu wala msiwe wavivu kunikumbuka.

44. Nendeni kwa Firauni, bila shaka amepita kiasi.

45. Na kamwambieni maneno laini, huenda atashika mawaidha au ataogopa.

46. Wakasema: Ee Mola wetu, hakika sisi tunaogopa asije kutufanyia matata au kutudhulumu.

47. Akasema: Msiogope, bila shaka Mimi ni pamoja nanyi: Nasikia na Naona.

48. Basi mwendeeni na mwambieni: Kwa yakini sisi ni Mitume wa Mola wako; kwa hiyo wapeleke pamoja nasi wana wa Israeli na usiwaadhibu. Hakika Tumekuletea Ishara itokayo kwa Mola wako, na amani iwe juu ya aufuataye mwongozo.

49. Hakika tumefunuliwa ya kwamba adhabu itamsibu yule akataaye na kugeuka.

إِذْ تَمْشِيٓ أُخْتُكَ فَتَقُولُ هَلْ أَدُلُّكُمْ
عَلَىٰ مَن يَكْفُلُهُۥ ۖ فَرَجَعْنَٰكَ إِلَىٰٓ أُمِّكَ
كَيْ تَقَرَّ عَيْنُهَا وَلَا تَحْزَنَ ۚ وَقَتَلْتَ
نَفْسًا فَنَجَّيْنَٰكَ مِنَ ٱلْغَمِّ وَفَتَنَّٰكَ
فُتُونًا ۚ فَلَبِثْتَ سِنِينَ فِىٓ أَهْلِ مَدْيَنَ ۙ
ثُمَّ جِئْتَ عَلَىٰ قَدَرٍ يَٰمُوسَىٰ ﴿٤٠﴾
وَٱصْطَنَعْتُكَ لِنَفْسِى ﴿٤١﴾
ٱذْهَبْ أَنتَ وَأَخُوكَ بِـَٔايَٰتِى وَلَا تَنِيَا
فِى ذِكْرِى ﴿٤٢﴾
ٱذْهَبَآ إِلَىٰ فِرْعَوْنَ إِنَّهُۥ طَغَىٰ ﴿٤٣﴾
فَقُولَا لَهُۥ قَوْلًا لَّيِّنًا لَّعَلَّهُۥ يَتَذَكَّرُ
أَوْ يَخْشَىٰ ﴿٤٤﴾
قَالَا رَبَّنَآ إِنَّنَا نَخَافُ أَن يَفْرُطَ عَلَيْنَآ
أَوْ أَن يَطْغَىٰ ﴿٤٥﴾
قَالَ لَا تَخَافَآ إِنَّنِى مَعَكُمَآ أَسْمَعُ
وَأَرَىٰ ﴿٤٦﴾
فَأْتِيَاهُ فَقُولَآ إِنَّا رَسُولَا رَبِّكَ فَأَرْسِلْ
مَعَنَا بَنِىٓ إِسْرَٰٓءِيلَ ۖ وَلَا تُعَذِّبْهُمْ ۖ
قَدْ جِئْنَٰكَ بِـَٔايَةٍ مِّن رَّبِّكَ ۖ وَٱلسَّلَٰمُ عَلَىٰ
مَنِ ٱتَّبَعَ ٱلْهُدَىٰٓ ﴿٤٧﴾
إِنَّا قَدْ أُوحِىَ إِلَيْنَآ أَنَّ ٱلْعَذَابَ عَلَىٰ
مَن كَذَّبَ وَتَوَلَّىٰ ﴿٤٨﴾

Aya 45. *Kamwambieni maneno laini.* Upole na ulainifu unafaa sana katika mazungumzo. Na mtu asiyeshika ulainifu wakati wa kutangaza haki mara nyingi hafanikiwi. Hivyo Mungu akawaambia Musa na Harun watumie upole na ulainifu wakati wa kuzungumza na Firauni isije akakasirika kabla ya kusikia neno la haki.

قَالَ فَمَنْ رَّبُّكُمَا يٰمُوْسٰى ﴿٥٠﴾

50. (Firauni) akasema: Mola wenu ni nani, ewe Musa?

قَالَ رَبُّنَا الَّذِيْٓ اَعْطٰى كُلَّ شَيْءٍ خَلْقَهٗ ثُمَّ هَدٰى ﴿٥١﴾

51. Akasema Mola wetu ni Yule Aliyekipa kila kitu umbo lake kisha Akakiongoza.

قَالَ فَمَا بَالُ الْقُرُوْنِ الْاُوْلٰى ﴿٥٢﴾

52. Akasema: Basi ni hali gani ya vizazi vya kwanza?

قَالَ عِلْمُهَا عِنْدَ رَبِّيْ فِيْ كِتٰبٍ ۚ لَا يَضِلُّ رَبِّيْ وَلَا يَنْسَى ﴿٥٣﴾

53. Akasema: Elimu yake iko kwa Mola wangu katika Kitabu. Mola wangu Hapotei wala Hasahau,

الَّذِيْ جَعَلَ لَكُمُ الْاَرْضَ مَهْدًا وَّسَلَكَ لَكُمْ فِيْهَا سُبُلًا وَّاَنْزَلَ مِنَ السَّمَآءِ مَآءً ؕ فَاَخْرَجْنَا بِهٖٓ اَزْوَاجًا مِّنْ نَّبَاتٍ شَتّٰى ﴿٥٤﴾

54. Ambaye Amewafanyieni ardhi kuwa tandiko na Akawawekeeni humo njia, na Akayateremsha maji kutoka mawinguni; na kwayo Tukaotesha namna nyingi za mimea mbalimbali.

كُلُوْا وَارْعَوْا اَنْعَامَكُمْ ؕ اِنَّ فِيْ ذٰلِكَ لَاٰيٰتٍ لِّاُولِي النُّهٰى ﴿٥٥﴾ ع ١١

55. Kuleni na walisheni wanyama wenu; bila shaka katika hayo zimo Ishara kwa wenye akili.

FUNGU 3

مِنْهَا خَلَقْنٰكُمْ وَفِيْهَا نُعِيْدُكُمْ وَمِنْهَا نُخْرِجُكُمْ تَارَةً اُخْرٰى ﴿٥٦﴾

56. Kwa (ardhi) hiyo Tumewaumbeni, na humo Tutawarudisheni, na toka humo Tutawatoeni mara nyingine.

وَلَقَدْ اَرَيْنٰهُ اٰيٰتِنَا كُلَّهَا فَكَذَّبَ وَاَبٰى ﴿٥٧﴾

57. Na hakika Tulimwonyesha Ishara Zetu zote lakini alikadhibisha na akakataa.

قَالَ اَجِئْتَنَا لِتُخْرِجَنَا مِنْ اَرْضِنَا بِسِحْرِكَ يٰمُوْسٰى ﴿٥٨﴾

58. Akasema: Umetujia kututoa katika nchi yetu kwa uchawi wako, ewe Musa?

فَلَنَاْتِيَنَّكَ بِسِحْرٍ مِّثْلِهٖ فَاجْعَلْ بَيْنَنَا وَبَيْنَكَ مَوْعِدًا لَّا نُخْلِفُهٗ نَحْنُ وَلَآ اَنْتَ مَكَانًا سُوًى ﴿٥٩﴾

59. Basi sisi tutakuletea uchawi mithili ya huo; kwa hiyo ufanye ahadi (ya mkutano) baina yetu na yako ambayo tusiivunje sisi wala wewe (katika) mahali patakapokuwa sawa.

Aya 58. Firauni aliposhindwa katika dalili na Ishara za kimbingu, akatumia hila nyingine ili apate kuwakasirisha watu wake juu ya Nabii Musa na Nabii Harun, yaani, akaanza kusema kuwa kusudi hasa la Musa na Harun si kutangaza habari za dini, bali wanataka kutufukuza katika nchi yetu na kunyang'anya mali zetu.

60. (Musa) akasema: Miadi yenu ni siku ya mapambo na watu wakusanywe asubuhi.

قَالَ مَوْعِدُكُمْ يَوْمُ الزِّيْنَةِ وَاَنْ يُّحْشَرَ النَّاسُ ضُحًى ﴿٦٠﴾

61. Kisha Firauni alienda zake na akakusanya hila zake zote kisha akaja mahali pa miadi.

فَتَوَلّٰى فِرْعَوْنُ فَجَمَعَ كَيْدَهٗ ثُمَّ اَتٰى ﴿٦١﴾

62. Musa akawaambia: Ole wenu! msizushe uwongo juu ya Allah, isije Akawafuteni kwa adhabu. Na amekwisha shindwa azushaye uwongo.

قَالَ لَهُمْ مُّوْسٰى وَيْلَكُمْ لَا تَفْتَرُوْا عَلَى اللّٰهِ كَذِبًا فَيُسْحِتَكُمْ بِعَذَابٍ ۚ وَقَدْ خَابَ مَنِ افْتَرٰى ﴿٦٢﴾

63. Basi wakazozana kwa shauri lao baina yao na wakashauriana kwa siri.

فَتَنَازَعُوْٓا اَمْرَهُمْ بَيْنَهُمْ وَ اَسَرُّوا النَّجْوٰى ﴿٦٣﴾

64. Wakasema: Hakika hawa wawili ni wachawi, wanataka kuwatoeni katika nchi yenu kwa uchawi wao, na kuondoa desturi yenu iliyo bora kabisa.

قَالُوْٓا اِنْ هٰذٰنِ لَسٰحِرٰنِ يُرِيْدٰنِ اَنْ يُّخْرِجٰكُمْ مِّنْ اَرْضِكُمْ بِسِحْرِهِمَا وَيَذْهَبَا بِطَرِيْقَتِكُمُ الْمُثْلٰى ﴿٦٤﴾

65. Kwa hiyo kusanyeni hila yenu, kisha mfike kwa kujipanga safu, na kwa yakini amestawi leo atakayeshinda.

فَاَجْمِعُوْا كَيْدَكُمْ ثُمَّ ائْتُوْا صَفًّا ۚ وَقَدْ اَفْلَحَ الْيَوْمَ مَنِ اسْتَعْلٰى ﴿٦٥﴾

66. Wakasema: Ewe Musa, je, utatupa au tutakuwa sisi wa kwanza kutupa?

قَالُوْا يٰمُوْسٰٓى اِمَّآ اَنْ تُلْقِيَ وَ اِمَّآ اَنْ نَّكُوْنَ اَوَّلَ مَنْ اَلْقٰى ﴿٦٦﴾

67. (Musa) akasema: Bali tupeni! Lo! kamba zao zikaonekana mbele yake, kwa uchawi wao, zikipiga mbio.

قَالَ بَلْ اَلْقُوْا ۚ فَاِذَا حِبَالُهُمْ وَعِصِيُّهُمْ يُخَيَّلُ اِلَيْهِ مِنْ سِحْرِهِمْ اَنَّهَا تَسْعٰى ﴿٦٧﴾

68. Basi Musa akaona hofu katika nafsi yake.

فَاَوْجَسَ فِيْ نَفْسِهٖ خِيْفَةً مُّوْسٰى ﴿٦٨﴾

Aya 62. Amekwisha shindwa azushaye uwongo. Historia ya wanadamu toka zamani, akili iliyo sahihi, na maisha ya Manabii wote waliokuja duniani vinashuhudia ya kuwa azushaye uwongo juu ya Mungu hawezi kamwe kufanikiwa.

Aya 64. *Kuondoa desturi yenu iliyo bora kabisa.* Makafiri siku zote wanasema maneno ya namna hii. Hutaka Manabii wa Allah wasivuruge desturi zao zilizo mbaya. Lakini hawafikiri kuwa Nabii wa Mungu haji ila kuondoa desturi za kishenzi na tabia za kishetani katika dunia. Kwa ajili hii wanalazimika kupinga desturi zote zilizo mbaya.

Aya 68. *Musa akaona hofu.* Nabii Musa hakuogopa kwa kufikiri kuwa wachawi wa Firauni

قُلْنَا لَا تَخَفْ اِنَّكَ اَنْتَ الْاَعْلٰى ﴿٦٨﴾

69. Tukasema: Usiogope, hakika wewe ndiwe mwenye kushinda.

وَاَلْقِ مَا فِيْ يَمِيْنِكَ تَلْقَفْ مَا صَنَعُوْا ؕ اِنَّمَا صَنَعُوْا كَيْدُ سٰحِرٍ ؕ وَلَا يُفْلِحُ السّٰحِرُ حَيْثُ اَتٰى ﴿٦٩﴾

70. Na kitupe kilicho katika mkono wako wa kuume: kitavimeza walivyovitengeneza; hakika wametengeneza hila za mchawi, wala mchawi hatafaulu po pote afikapo.

فَاُلْقِيَ السَّحَرَةُ سُجَّدًا قَالُوْٓا اٰمَنَّا بِرَبِّ هٰرُوْنَ وَمُوْسٰى ﴿٧٠﴾

71. Basi wachawi wakaangushwa kusujudu, wakisema: Tumemwamini Mola wa Harun na Musa.

قَالَ اٰمَنْتُمْ لَهٗ قَبْلَ اَنْ اٰذَنَ لَكُمْ ؕ اِنَّهٗ لَكَبِيْرُكُمُ الَّذِيْ عَلَّمَكُمُ السِّحْرَ ۚ فَلَاُقَطِّعَنَّ اَيْدِيَكُمْ وَاَرْجُلَكُمْ مِّنْ خِلَافٍ وَّلَاُصَلِّبَنَّكُمْ فِيْ جُذُوْعِ النَّخْلِ ۫ وَلَتَعْلَمُنَّ اَيُّنَآ اَشَدُّ عَذَابًا وَّاَبْقٰى ﴿٧١﴾

72. (Firauni) akasema: Je, mnamwamini kabla sijawapeni ruhusa! Bila shaka yeye ndiye mkubwa wenu aliyewafunzeni uchawi. Kwa hiyo, hakika nitawakateni mikono yenu na miguu yenu kwa kutofautisha na kwa yakini nitawaueni kwa kuwawamba katika mashina ya mitende, na bila shaka mtajua ni nani wetu aliye mkali wa kuadhibu na mwenye kuendelea kubaki.

قَالُوْا لَنْ نُّؤْثِرَكَ عَلٰى مَا جَآءَنَا مِنَ الْبَيِّنٰتِ وَالَّذِيْ فَطَرَنَا فَاقْضِ مَآ اَنْتَ قَاضٍ ؕ اِنَّمَا تَقْضِيْ هٰذِهِ الْحَيٰوةَ الدُّنْيَا ﴿٧٢﴾

73. Wakasema: Hatukutangulizi kamwe juu ya Ishara waziwazi zilizotufikia, na juu ya Yule Aliyetuumba, basi fanya unavyotaka kufanya; unaweza kutoa hukumu inayohusiana na maisha haya ya dunia tu.

اِنَّآ اٰمَنَّا بِرَبِّنَا لِيَغْفِرَ لَنَا خَطٰيٰنَا وَمَآ اَكْرَهْتَنَا عَلَيْهِ مِنَ السِّحْرِ ؕ وَاللّٰهُ خَيْرٌ وَّاَبْقٰى ﴿٧٣﴾

74. Kwa yakini tumemwamini Mola wetu ili Atusamehe makosa yetu na uchawi ule uliotushurutisha; na Allah ndiye Mbora na Adumuye.

اِنَّهٗ مَنْ يَّاْتِ رَبَّهٗ مُجْرِمًا فَاِنَّ لَهٗ جَهَنَّمَ ؕ لَا يَمُوْتُ فِيْهَا وَلَا يَحْيٰى ﴿٧٤﴾

75. Hakika atakayekuja kwa Mola wake hali yu mkosefu, basi kwa yakini atapata Jahanamu; hatakufa humo wala hataishi.

watamshinda . La, Nabii hawezi kufikiri kuwa atashindwa na waganga. Bali hofu yake ilikuwa juu ya watu kwamba isije wakadanganyika kwa kamba za wachawi na wakashindwa kupambanua baina ya haki na batili, maana hakujua kama fimbo yake itameza mazingaombwe ya wale wachawi.

76. Na atakayemjia hali yu mumini amefanya vitendo vizuri, basi hao ndio watakaopata vyeo vya juu.

وَمَنْ يَّاْتِهٖ مُؤْمِنًا قَدْ عَمِلَ الصّٰلِحٰتِ فَاُولٰٓئِكَ لَهُمُ الدَّرَجٰتُ الْعُلٰى ۙ﴿۷۶﴾

77. Bustani za milele zipitazo mito ndani yao, wakikaa humo. Na hayo ni malipo ya mwenye kujitakasa.

جَنّٰتُ عَدْنٍ تَجْرِيْ مِنْ تَحْتِهَا الْاَنْهٰرُ خٰلِدِيْنَ فِيْهَا ؕ وَذٰلِكَ جَزٰٓؤُا مَنْ تَزَكّٰى ﴿۷۷﴾ ع ۱۳

FUNGU 4

78. Na hakika Tulimfunulia Musa kwamba wapeleke usiku usiku watumishi Wangu, na ukawafanyie njia kavu baharini; usiogope kukamatwa wala usiogope lo lote.

وَلَقَدْ اَوْحَيْنَآ اِلٰى مُوْسٰٓى ۙ اَنْ اَسْرِ بِعِبَادِيْ فَاضْرِبْ لَهُمْ طَرِيْقًا فِي الْبَحْرِ يَبَسًا ۙ لَّا تَخٰفُ دَرَكًا وَّلَا تَخْشٰى ﴿۷۸﴾

79. Basi Firauni akawafuata pamoja na majeshi yake, na kikawafunikiza katika bahari kilichowafunikiza.

فَاَتْبَعَهُمْ فِرْعَوْنُ بِجُنُوْدِهٖ فَغَشِيَهُمْ مِّنَ الْيَمِّ مَا غَشِيَهُمْ ﴿۷۹﴾

80. Na Firauni akawapoteza watu wake wala hakuwaongoza.

وَاَضَلَّ فِرْعَوْنُ قَوْمَهٗ وَمَا هَدٰى ﴿۸۰﴾

81. Enyi wana wa Israeli! hakika Tumewaokoeni na adui yenu na Tukawaahidini upande wa kuume wa mlima na Tukawateremshieni Manna na Salwa:

يٰبَنِيْٓ اِسْرَآءِيْلَ قَدْ اَنْجَيْنٰكُمْ مِّنْ عَدُوِّكُمْ وَوٰعَدْنٰكُمْ جَانِبَ الطُّوْرِ الْاَيْمَنَ وَنَزَّلْنَا عَلَيْكُمُ الْمَنَّ وَالسَّلْوٰى ﴿۸۱﴾

82. Kuleni katika vitu vizuri Tulivyokuruzukuni wala msiiruke mipaka katika hivyo isije ikawashukieni ghadhabu Yangu. Na inayemshukia ghadhabu Yangu, basi ameangamia.

كُلُوْا مِنْ طَيِّبٰتِ مَا رَزَقْنٰكُمْ وَلَا تَطْغَوْا فِيْهِ فَيَحِلَّ عَلَيْكُمْ غَضَبِيْ ۚ وَمَنْ يَّحْلِلْ عَلَيْهِ غَضَبِيْ فَقَدْ هَوٰى ﴿۸۲﴾

83. Na hakika Mimi ni Msamehevu sana kwa anayetubia na kuamini na kutenda mema, tena ashikaye mwongozo.

وَاِنِّيْ لَغَفَّارٌ لِّمَنْ تَابَ وَاٰمَنَ وَعَمِلَ صَالِحًا ثُمَّ اهْتَدٰى ﴿۸۳﴾

84. Na nini kimekuharakisha kwa kuwaacha watu wako, ewe Musa?

وَمَآ اَعْجَلَكَ عَنْ قَوْمِكَ يٰمُوْسٰى ﴿۸۴﴾

85. Akasema: Wako nyuma yangu wananifuata; na nimeharakia Kwako, Mola wangu, ili Uwe radhi.

قَالَ هُمْ اُولَآءِ عَلٰٓى اَثَرِيْ وَعَجِلْتُ اِلَيْكَ رَبِّ لِتَرْضٰى ﴿۸۵﴾

قَالَ فَاِنَّا قَدْ فَتَنَّا قَوْمَكَ مِنْۢ بَعْدِكَ وَاَضَلَّهُمُ السَّامِرِيُّ ﴿٨٥﴾

86. (Mungu) Akasema: Bila shaka Tumewajaribu watu wako baada yako, na Samiri amewapoteza.

فَرَجَعَ مُوْسٰٓى اِلٰى قَوْمِهٖ غَضْبَانَ اَسِفًا ۚ قَالَ يٰقَوْمِ اَلَمْ يَعِدْكُمْ رَبُّكُمْ وَعْدًا حَسَنًا ۭ اَفَطَالَ عَلَيْكُمُ الْعَهْدُ اَمْ اَرَدْتُّمْ اَنْ يَّحِلَّ عَلَيْكُمْ غَضَبٌ مِّنْ رَّبِّكُمْ فَاَخْلَفْتُمْ مَّوْعِدِيْ ﴿٨٦﴾

87. Basi Musa akarudi kwa watu wake kwa ghadhabu akisikitika. Akasema: Enyi watu wangu, je, Mola wenu Hakuwaahidini ahadi nzuri? Je, imekuwa ndefu kwenu ahadi hiyo au mmetaka iwashukieni ghadhabu kutoka kwa Mola wenu; na kwa hiyo mmevunja ahadi yangu?

قَالُوْا مَآ اَخْلَفْنَا مَوْعِدَكَ بِمَلْكِنَا وَلٰكِنَّا حُمِّلْنَآ اَوْزَارًا مِّنْ زِيْنَةِ الْقَوْمِ فَقَذَفْنٰهَا فَكَذٰلِكَ اَلْقَى السَّامِرِيُّ ﴿٨٧﴾

88. Wakasema: Sisi hatukuvunja ahadi yako kwa hiyari yetu, walakini tulibebeshwa mizigo ya mapambo ya watu, tukaitupa (motoni) na hivyo ndivyo alivyotia Samiri.

فَاَخْرَجَ لَهُمْ عِجْلًا جَسَدًا لَّهٗ خُوَارٌ فَقَالُوْا هٰذَآ اِلٰهُكُمْ وَاِلٰهُ مُوْسٰى ۡ فَنَسِيَ ﴿٨٨﴾

89. Kisha akawatolea ndama - kiwiliwili tu kilichokuwa kikitoa sauti ya chini-chini. Kisha yeye na masahaba zake wakasema: Huyu ndiye Mungu wenu na Mungu wa Musa lakini yeye alisahau kumtambulisha kwenu.

اَفَلَا يَرَوْنَ اَلَّا يَرْجِعُ اِلَيْهِمْ قَوْلًا ۙ وَّلَا يَمْلِكُ لَهُمْ ضَرًّا وَّلَا نَفْعًا ﴿٨٩﴾ ع ١٣

90. Je, hawakuona ya kuwa hakuwarudishia neno wala hakuwamilikia dhara wala nufaa?

FUNGU 5

وَلَقَدْ قَالَ لَهُمْ هٰرُوْنُ مِنْ قَبْلُ يٰقَوْمِ اِنَّمَا فُتِنْتُمْ بِهٖ ۚ وَاِنَّ رَبَّكُمُ الرَّحْمٰنُ

91. Na bila shaka Harun alikwisha waambia zamani, Enyi watu wangu! Hakika ninyi mmefitinishwa tu kwa kitu

Aya 90. Hapa uungu wa ndama wa Samiri unakataliwa na Allah kwa dalili ya kutosema kwake. Kusema ndiyo dalili ya kutuonyesha kuwa Mungu yuko. Watu wanaofikiri kuwa Mungu alikuwa anasema na watu wa zamani tu na siku hizi hasemi tena wamedanganyika vibaya sana; na Aya hii ni dalili ya wazi ya kubatilisha fikira hizo. Bila shaka Mungu leo pia anasema na wale ambao anawapenda kama alivyokuwa akizungumza zamani na wapenzi Wake. Mlango wa wahyi na ufunuo ni mlango ulio wazi daima.

Aya 91. Biblia inaeleza ya kuwa Nabii Harun ndiye aliyewafanyia Waisraeli huyo ndama wapate kumwabudu (Kutoka 32:1-6). Ni wazi ya kuwa kusema hivyo si kweli. Haiwezekani

فَاتَّبِعُوْنِيْ وَاَطِيْعُوْٓا اَمْرِيْ ﴿٩١﴾

hiki na kwa yakini Mola wenu ni Mungu wa rehema, basi nifuateni na tiini amri yangu.

قَالُوْا لَنْ نَّبْرَحَ عَلَيْهِ عٰكِفِيْنَ حَتّٰى يَرْجِعَ اِلَيْنَا مُوْسٰى ﴿٩٢﴾

92. Wakasema: Hatutaacha kabisa kukiabudu mpaka Musa aturudie.

قَالَ يٰهٰرُوْنُ مَا مَنَعَكَ اِذْ رَاَيْتَهُمْ ضَلُّوْٓا ﴿٩٣﴾

93. (Musa) akasema: Ewe Harun, ni nini kilichokuzuia ulipowaona wakipotea.

اَلَّا تَتَّبِعَنِ ؕ اَفَعَصَيْتَ اَمْرِيْ ﴿٩٤﴾

94. Ili usinifuate; je, umeasi amri yangu?

قَالَ يَبْنَؤُمَّ لَا تَاْخُذْ بِلِحْيَتِيْ وَلَا بِرَاْسِيْ ۚ اِنِّيْ خَشِيْتُ اَنْ تَقُوْلَ فَرَّقْتَ بَيْنَ بَنِيْٓ اِسْرَآءِيْلَ وَلَمْ تَرْقُبْ قَوْلِيْ ﴿٩٥﴾

95. Akasema: Ewe mwana wa mama yangu, usinikamate kwa ndevu zangu wala kwa nywele za kichwa changu. Mimi niliogopa usije ukasema: Umesababisha mfarakano miongoni mwa wana wa Israeli, na hukusubiri kauli yangu.

قَالَ فَمَا خَطْبُكَ يٰسَامِرِيُّ ﴿٩٦﴾

96. (Musa) akasema: Ewe Samiri, basi nia yako ilikuwa nini?

Nabii wa Mungu aliyesikia maneno ya Mungu kufanya jambo la namna hiyo. Mtu aliyeona jua hawezi kulidhani ni mshumaa; au aliyeona tembo hawezi kuona panya akafikiri ndiye tembo; mtu anayemwona mtu mwingine hawezi kumfananisha na funza. Hivyo haiwezekani kwa Mtume wa Mungu aliyemwona Mungu kwa macho ya roho na kumsikia sauti Yake, kufanya ndama wa dhahabu na kumwabudu. Inaonekana watu walioingiza maneno ya namna hii katika Biblia walikuwa wajinga kupita kiasi. Mfalme wa desturi tu hangependa kuchagua Gavana mpumbavu. Biblia inakubali ya kuwa Mungu anajua habari za mioyo ya watu. Basi Mungu angewezaje kumchagua mtu kuwa Nabii na kuwaongoza Waisraeli ambaye baadaye, atapinduka na kuwa anayeabudu sanamu? Je, hawa walioingiza maneno namna hii katika Biblia, walikuwa ni watu na akili zao?

Aliyewapoteza Waisraeli ni mtu aliyeitwa Samiri. Padre Dale, kwa kupofushwa na uadui, amesema maneno ya upumbavu kabisa juu ya habari za huyu Samiri. Ameandika, "Watu watatu watajwa katika sura hii, Samiri, Haman na Farao . . . Inaelekea kuwa Samiri huyu alidhaniwa kuwa Msamaria, maana Muhammad hakujua kuwa Samaria haukujengwa ila miaka mingi sana baada ya zamani za Musa" (uk. 631).

Kilichomfanya padre huyo adhanie huyu Samiri ni Msamaria, si kingine ila uadui wa kishenzi alio nao. Anakari mwenyewe kuwa Samiri ni mmoja katika watu watatu waliotajwa katika sura, na ambao ni wazi walikuwako katika majira moja. Hakuna mahali po pote katika Qur'an au Hadithi panapoeleza ya kuwa Samiri si jina la mtu bali la kabila. Lingekuwa ni jina la kabila, basi na Haman pia na Farao yangekuwa majina ya makabila. Lakini sivyo. Hayo yote ni majina ya watu maalum waliokuwako. Shauku yake ya kijinga inampoteza, naye anajaribu kupoteza watu wengine, kwa namna mbaya kabisa.

قَالَ بَصُرْتُ بِمَا لَمْ يَبْصُرُوْا بِهٖ فَقَبَضْتُ
قَبْضَةً مِّنْ اَثَرِ الرَّسُوْلِ فَنَبَذْتُهَا
وَكَذٰلِكَ سَوَّلَتْ لِيْ نَفْسِيْ ﴿٩٧﴾

97. Akasema: Niliona wasiyoyaona na nikashika sehemu chache ya mwendo wa Mtume, kisha nikautupa: na hivi ndivyo ilinielekeza nafsi yangu.

قَالَ فَاذْهَبْ فَاِنَّ لَكَ فِي الْحَيٰوةِ اَنْ
تَقُوْلَ لَا مِسَاسَ ۖ وَاِنَّ لَكَ مَوْعِدًا لَّنْ
تُخْلَفَهٗ ۚ وَانْظُرْ اِلٰٓى اِلٰهِكَ الَّذِيْ
ظَلْتَ عَلَيْهِ عَاكِفًا ۭ لَنُحَرِّقَنَّهٗ ثُمَّ
لَنَنْسِفَنَّهٗ فِي الْيَمِّ نَسْفًا ﴿٩٨﴾

98. (Musa) akasema: Basi ondoka, na kwa yakini itakuwa kwako katika maisha kusema: Usiniguse; na bila shaka ni ahadi kwako isiyovunjwa. Na ukamtazame mungu uliyeendelea kumwabudu, bila shaka tutamteketeza (kwa moto) kisha tutamsambaza katika bahari kwa msambazo.

اِنَّمَآ اِلٰهُكُمُ اللّٰهُ الَّذِيْ لَآ اِلٰهَ اِلَّا هُوَ ۭ
وَسِعَ كُلَّ شَيْءٍ عِلْمًا ﴿٩٩﴾

99. Hakika mwabudiwa wenu ni Allah tu, Ambaye hakuna aabudiwaye ila Yeye. Amekienea kila kitu kwa elimu.

كَذٰلِكَ نَقُصُّ عَلَيْكَ مِنْ اَنْۢبَاۗءِ مَا
قَدْ سَبَقَ ۚ وَقَدْ اٰتَيْنٰكَ مِنْ لَّدُنَّا ذِكْرًا ﴿١٠٠﴾ۖ

100. Kadhalika Tunakuhadithia katika habari za (mambo) yaliyotangulia, na bila shaka Tumekupa mawaidha kutoka Kwetu.

مَنْ اَعْرَضَ عَنْهُ فَاِنَّهٗ يَحْمِلُ يَوْمَ الْقِيٰمَةِ
وِزْرًا ﴿١٠١﴾ۙ

101. Atakayejitenga mbali nayo, basi kwa yakini atabeba siku ya Kiyama mzigo.

Aya 95. Maneno *usinikamate kwa ndevu zangu, wala kwa (nywele za) kichwa changu* yasichukuliwe kwa tafsiri ya neno kwa neno. Yanaweza tu kuwa na maana ya usinidhalilishe.

Pia Tazama sura 7:151.

Aya 97. Samiri alipoulizwa atoe sababu ya kosa lake, anajibu vile anavyojibu mwizi anayekamatwa katika hali ya kuiba na asiweze kukataa. Anasema: Ndiyo nilimfuata Mtume (Musa) kidogo na nikakiri Umoja wa Mungu. Lakini baadaye nikakataa, na sasa sitaki. *Hivi ndivyo nafsi yangu ilivyonielekeza.* Kwa kuwa majibu haya ya Samiri yanaonyesha uchafu wa moyo wake, Nabii Musa akamjibu ya kuwa kama ni hivyo ajue ya kuwa hali yake itakuwa mbaya katika dunia na Akhera na yeye mwenyewe atawafanya watu wasimsogelee, na wamkimbie.

Aya 100. Baada ya kueleza habari za Nabii Musa, Allah anamrudia Mtume s.a.w. kumwambia kuwa habari hizi hazikuelezwa hapa kwa namna ya kisa, bali ni habari zitakazokupitia wewe pia. Utapita katika njia zile zile alizopita Nabii Musa, na mwishoni majabari na mafirauni wataangamia, nawe utafanikiwa.

Mtume *s.a.w.* alitangaza habari hizi alipokuwa katika hali ya taabu katika Makka, na tunaona ya kuwa mwishoni alifanikiwa, na maadui zake wakaangamia.

خٰلِدِيْنَ فِيْهِ ؕ وَ سَآءَ لَهُمْ يَوْمَ الْقِيٰمَةِ حِمْلًا ﴿۱۰۲﴾

102. Wakikaa humo, na vibaya kwao siku ya Kiyama kubeba mzigo.

يَّوْمَ يُنْفَخُ فِي الصُّوْرِ وَ نَحْشُرُ الْمُجْرِمِيْنَ يَوْمَئِذٍ زُرْقًا ﴿۱۰۳﴾

103. Siku itakayopigwa baragumu na Tutawakusanya wakosefu siku hiyo hali macho yao yatakuwa ya kibuluu.

يَّتَخَافَتُوْنَ بَيْنَهُمْ اِنْ لَّبِثْتُمْ اِلَّا عَشْرًا ﴿۱۰۴﴾

104. Watanong'onezana wao kwa wao: Hamkukaa ila (siku) kumi tu.

نَحْنُ اَعْلَمُ بِمَا يَقُوْلُوْنَ اِذْ يَقُوْلُ اَمْثَلُهُمْ طَرِيْقَةً اِنْ لَّبِثْتُمْ اِلَّا يَوْمًا ﴿۱۰۵﴾ ع

105. Sisi Tunajua sana watakayosema, atakaposema mbora wao katika mwendo: Ninyi hamkukaa ila siku moja tu.

FUNGU 6

وَ يَسْـَٔلُوْنَكَ عَنِ الْجِبَالِ فَقُلْ يَنْسِفُهَا رَبِّيْ نَسْفًا ﴿۱۰۶﴾

106. Na wanakuuliza habari za milima. Basi sema: Mola wangu Ataivunja vunja kabisa .

فَيَذَرُهَا قَاعًا صَفْصَفًا ﴿۱۰۷﴾

107. Na Ataiacha uwanda mtambarare,

لَّا تَرٰى فِيْهَا عِوَجًا وَّ لَاۤ اَمْتًا ﴿۱۰۸﴾

108. Hutaona humo kombo wala miinuko.

يَوْمَئِذٍ يَّتَّبِعُوْنَ الدَّاعِيَ لَا عِوَجَ لَهٗ ۚ وَ خَشَعَتِ الْاَصْوَاتُ لِلرَّحْمٰنِ فَلَا تَسْمَعُ اِلَّا هَمْسًا ﴿۱۰۹﴾

109. Siku hiyo watamfuata mwitaji aliye imara na asiye na upotevu; na sauti zote zitanyamazishwa mbele ya Allah Aliye Mwingi wa Huruma na hutasikia ila minong'ono.

يَوْمَئِذٍ لَّا تَنْفَعُ الشَّفَاعَةُ اِلَّا مَنْ اَذِنَ لَهُ الرَّحْمٰنُ وَ رَضِيَ لَهٗ قَوْلًا ﴿۱۱۰﴾

110. Siku hiyo hautafaa uombezi ila kwa yule Anayemruhusu Mungu wa huruma na kuiridhia kauli yake.

يَعْلَمُ مَا بَيْنَ اَيْدِيْهِمْ وَ مَا خَلْفَهُمْ وَ لَا يُحِيْطُوْنَ بِهٖ عِلْمًا ﴿۱۱۱﴾

111. Anajua yaliyo mbele yao na yaliyo nyuma yao, wala hawamzunguki kwa elimu.

Aya 106. *Milima.* Milima ni watu wakubwa-wakubwa. Watu walimwuliza Mtume s.a.w. itakuwaje hali ya hao wakubwa wa nchi kama Abu Jahal, Utba, Walid na wengineo. Allah anasema: Uwaambie Mungu atawaondoa kabisa katika njia ya dini ya Kiislamu hata haitajulikana wamekwenda wapi. Ndivyo ilivyotokea. Maadui wote wakubwa-wakubwa wa dini ya Kiislamu waliangamia na sasa majina yao yamebaki visa tu, hali Uislamu unaendelea kuenea kila upande na heshima ya Mtume *s.a.w.* inazidi.

وَعَنَتِ الْوُجُوْهُ لِلْحَيِّ الْقَيُّوْمِ ؕ وَقَدْ خَابَ مَنْ حَمَلَ ظُلْمًا ﴿۱۱۲﴾

112. Na nyuso zitainama mbele ya Aliye Hai, Mzima wa milele; na ameshindwa aliyefanya dhuluma.

وَمَنْ يَّعْمَلْ مِنَ الصّٰلِحٰتِ وَهُوَ مُؤْمِنٌ فَلَا يَخٰفُ ظُلْمًا وَّلَا هَضْمًا ﴿۱۱۳﴾

113. Na atakayefanya vitendo vizuri, naye ni mumini, basi hataogopa dhuluma wala kunyimwa.

وَكَذٰلِكَ اَنْزَلْنٰهُ قُرْاٰنًا عَرَبِيًّا وَّصَرَّفْنَا فِيْهِ مِنَ الْوَعِيْدِ لَعَلَّهُمْ يَتَّقُوْنَ اَوْ يُحْدِثُ لَهُمْ ذِكْرًا ﴿۱۱۴﴾

114. Na ndivyo Tulivyoiteremsha Qur'an kwa Kiarabu - na Tumeeleza humo mara kwa mara maonyo ili wapate kumcha Allah au kwamba ili iwadhihirishie ishara ionyayo.

فَتَعٰلَى اللّٰهُ الْمَلِكُ الْحَقُّ ۚ وَلَا تَعْجَلْ بِالْقُرْاٰنِ مِنْ قَبْلِ اَنْ يُّقْضٰۤى اِلَيْكَ وَحْيُهٗ ۫ وَقُلْ رَّبِّ زِدْنِيْ عِلْمًا ﴿۱۱۵﴾

115. Basi Atukuzwaye ni Allah, Mfalme wa haki. Wala usifanye haraka kwa Qur'an, kabla haujamalizika kukufikia ufunuo wake, na uombe: Mola wangu, nizidishie elimu.

وَلَقَدْ عَهِدْنَاۤ اِلٰۤى اٰدَمَ مِنْ قَبْلُ فَنَسِيَ وَلَمْ نَجِدْ لَهٗ عَزْمًا ﴿۱۱۶﴾ ع ۱۵

116. Na bila shaka Tulimwahidi Adamu zamani, basi akasahau, lakini Hatukumwona mwenye nia (ya kuvunja ahadi).

FUNGU 7

وَاِذْ قُلْنَا لِلْمَلٰٓئِكَةِ اسْجُدُوْا لِاٰدَمَ فَسَجَدُوْۤا اِلَّاۤ اِبْلِيْسَ ؕ اَبٰى ﴿۱۱۷﴾

117. Na (kumbukeni) Tulipowaambia Malaika, Mtiini Adamu, basi wakatii isipokuwa Ibilisi, alikana.

فَقُلْنَا يٰۤاٰدَمُ اِنَّ هٰذَا عَدُوٌّ لَّكَ وَلِزَوْجِكَ فَلَا يُخْرِجَنَّكُمَا مِنَ الْجَنَّةِ فَتَشْقٰى ﴿۱۱۸﴾

118. Basi Tukasema: Ewe Adamu, hakika huyu ni adui yako na ya mke wako, hivyo asiwatoeni katika bustani mkaingia taabuni.

اِنَّ لَكَ اَلَّا تَجُوْعَ فِيْهَا وَلَا تَعْرٰى ﴿۱۱۹﴾

119. Hakika hutakuwa mwenye njaa humo wala hutakuwa uchi.

وَاَنَّكَ لَا تَظْمَؤُا فِيْهَا وَلَا تَضْحٰى ﴿۱۲۰﴾

120. Na kwa yakini hutapata kiu humo wala hutapata joto.

فَوَسْوَسَ اِلَيْهِ الشَّيْطٰنُ قَالَ يٰۤاٰدَمُ هَلْ اَدُلُّكَ عَلٰى شَجَرَةِ الْخُلْدِ وَمُلْكٍ لَّا يَبْلٰى ﴿۱۲۱﴾

121. Basi Shetani akamtia wasiwasi; akamwambia: Ewe Adamu, je, nikujulishe mti wa milele na ufalme usiokoma?

فَاَكَلَا مِنْهَا فَبَدَتْ لَهُمَا سَوْاٰتُهُمَا وَطَفِقَا يَخْصِفٰنِ عَلَيْهِمَا مِنْ وَّرَقِ الْجَنَّةِ ۛ وَعَصٰۤى اٰدَمُ رَبَّهٗ فَغَوٰى ﴿۱۲۱﴾

122. Ndipo wakaula wote wawili na udhaifu wao wa asili ukawadhihirikia. Kwa hiyo wakaanza kujifunika kwa majani kutoka katika bustani. Na Adamu hakumtii Mola wake na Adamu akaacha njia na kwenda upande.

ثُمَّ اجْتَبٰهُ رَبُّهٗ فَتَابَ عَلَيْهِ وَ هَدٰى ﴿۱۲۲﴾

123. Kisha Mola wake Akamchagua na Akamwelekea na Akamwongoza.

قَالَ اهْبِطَا مِنْهَا جَمِيْعًا ۚ بَعْضُكُمْ لِبَعْضٍ عَدُوٌّ ۚ فَاِمَّا يَاْتِيَنَّكُمْ مِّنِّيْ هُدًى ۙ فَمَنِ اتَّبَعَ هُدَايَ فَلَا يَضِلُّ وَلَا يَشْقٰى ﴿۱۲۳﴾

124. Akasema: Ondokeni humo nyote m maadui ninyi kwa ninyi; na kama ukiwafikieni kutoka Kwangu mwongozo, basi atakayeufuata mwongozo Wangu hatapotea wala hatakuwa na bahati mbaya.

وَمَنْ اَعْرَضَ عَنْ ذِكْرِيْ فَاِنَّ لَهٗ مَعِيْشَةً ضَنْكًا وَّ نَحْشُرُهٗ يَوْمَ الْقِيٰمَةِ اَعْمٰى ﴿۱۲۴﴾

125. Na atakayejiepusha kunikumbuka, basi kwa yakini atapata maisha yenye dhiki, na siku ya Kiyama Tutamfufua hali yu kipofu.

قَالَ رَبِّ لِمَ حَشَرْتَنِيْۤ اَعْمٰى وَقَدْ كُنْتُ بَصِيْرًا ﴿۱۲۵﴾

126. Atasema: Ee Mola wangu, mbona Umenifufua kipofu na hali nilikuwa nikiona?

Aya 122. Wafasiri wengi wamelichukulia jambo hili kwa kiwango kikubwa sana katika maana yake ya neno kwa neno wakati kuna ushahidi wa kutosha ndani ya maandiko haya wa kukanusha matumizi ya nano kwa neno. Dhambi inayozungumziwa ni dhahiri kabisa kwamba inahusiana na msepetuko uliotokea ndani ya mwili kama inavyobainishwa na ile sehemu ya aya inayotangaza kwamba ule udhaifu wao *sau'aatuhumaa* ukajulikana kwao. Kama ungelikuwa uchi wa kimwili yawezekanaje uwe hawakuujua uchi wao huo tokea siku waliyozaliwa hadi wakati wa tukio lile?

Kwa hiyo ni dhahiri kwamba Qur'an Tukufu inanasibishwa kimakosa na maana ya neno kwa neno. Kiasili neno *sau'aa* linatumika kwa vitendo vya aibu na vyenye welekea wa kutenda maovu. Wakati wa kutenda kosa mkosefu anagundua udhaifu wake uliojificha kutokana na hofu aipatayo. Udhaifu huu ni wa kisaikolojia na uko ndani ya mwili, wenye kuhusiana na akili na moyo, na hauwezi kufunikwa na kufichwa kwa kubandika majani mwilini mwa mtu. Hivyo basi kwa maana halisi ya kosa hili, lo lote liwalo, ambalo Adamu na Eva walilitenda, kufunika kutakuwa na maana tu ya kuomba msamaha kutoka kwa Allah na (kuomba ulinzi kutoka kwa Allah). Kwa maana hiyo basi majani ya bustani ni lazima yaeleweke kimethali kwa maana ya kutafuta kimbilio chini ya msamaha wa Allah na hicho ndicho alichofanya Adamu kwa mujibu wa Qur'an ambamo imetajwa waziwazi kwamba Allah Mwenyewe Alimfundisha yale maneno ambayo yangemwondolea athari za makosa yake na kwa kuyaitikia maneno yale Allah Alimwelekea kwa rehema na usamehevu.

قَالَ كَذٰلِكَ اَتَتْكَ اٰيٰتُنَا فَنَسِيْتَهَا ۚ وَكَذٰلِكَ الْيَوْمَ تُنْسٰى ﴿١٢٧﴾

127. (Mungu) Atasema: Hivyo ndivyo zilikufikia Aya Zetu lakini ukazisahau, na kadhalika leo utasahauliwa.

وَكَذٰلِكَ نَجْزِيْ مَنْ اَسْرَفَ وَلَمْ يُؤْمِنْۢ بِاٰيٰتِ رَبِّهٖ ؕ وَلَعَذَابُ الْاٰخِرَةِ اَشَدُّ وَاَبْقٰى ﴿١٢٨﴾

128. Na hivi ndivyo Tutakavyomlipa apitaye kiasi na asiyeamini Aya za Mola wake; na bila shaka adhabu ya Akhera ni kali zaidi na iendeleayo sana.

اَفَلَمْ يَهْدِ لَهُمْ كَمْ اَهْلَكْنَا قَبْلَهُمْ مِّنَ الْقُرُوْنِ يَمْشُوْنَ فِيْ مَسٰكِنِهِمْ ؕ اِنَّ فِيْ ذٰلِكَ لَاٰيٰتٍ لِّاُولِي النُّهٰى ﴿١٢٩﴾ ع ١٢

129. Je, haikuwaongoza ni vizazi vingapi Tulivyoviangamiza kabla yao, waliokuwa wakitembea katika maskani zao? Bila shaka katika hayo zimo Ishara kwa wenye akili.

FUNGU 8

وَلَوْلَا كَلِمَةٌ سَبَقَتْ مِنْ رَّبِّكَ لَكَانَ لِزَامًا وَّاَجَلٌ مُّسَمًّى ﴿١٣٠﴾

130. Na kama lisingelikuwa neno lililotangulia kutoka kwa Mola wako, na muda uliokwishawekwa, adhabu yao ingalikuwa ya kudumu.

فَاصْبِرْ عَلٰى مَا يَقُوْلُوْنَ وَسَبِّحْ بِحَمْدِ رَبِّكَ قَبْلَ طُلُوْعِ الشَّمْسِ وَقَبْلَ غُرُوْبِهَا ۚ وَمِنْ اٰنَآئِ الَّيْلِ فَسَبِّحْ وَاَطْرَافَ النَّهَارِ لَعَلَّكَ تَرْضٰى ﴿١٣١﴾

131. Basi yavumilie hayo wayasemayo, na utukuze kwa sifa za Mola wako kabla halijatoka jua na kabla halijatua, na nyakati za usiku pia umtukuze, na katikati ya mchana, ili uridhike.

وَلَا تَمُدَّنَّ عَيْنَيْكَ اِلٰى مَا مَتَّعْنَا بِهٖۤ اَزْوَاجًا مِّنْهُمْ زَهْرَةَ الْحَيٰوةِ الدُّنْيَا ۙ لِنَفْتِنَهُمْ فِيْهِ ؕ وَرِزْقُ رَبِّكَ خَيْرٌ وَّاَبْقٰى ﴿١٣٢﴾

132. Wala usivikodolee macho yako Tulivyowafaidisha watu wengi miongoni mwao: ni mapambo ya maisha ya dunia, ili Tuwajaribu kwavyo; na riziki ya Mola wako (Akupayo) ni bora mno na iendeleayo sana.

وَاْمُرْ اَهْلَكَ بِالصَّلٰوةِ وَاصْطَبِرْ عَلَيْهَا ؕ لَا نَسْـَٔلُكَ رِزْقًا ؕ نَحْنُ نَرْزُقُكَ ؕ وَالْعَاقِبَةُ لِلتَّقْوٰى ﴿١٣٣﴾

133. Na uwaamuru ahali zako kusali, na uendelee kwa hayo; Hatukuombi riziki bali sisi Tunakuruzuku, na mwisho mwema ni kwa (washikao) ucha-Mungu.

134. Na wakasema: Kwa nini hakutuletea Ishara kutoka kwa Mola wake? Je, haikuwafikia dalili wazi ya yale yaliyokuwa katika Vitabu vya kale?

وَقَالُوْا لَوْلَا يَاْتِيْنَا بِاٰيَةٍ مِّنْ رَّبِّهٖ ؕ اَوَلَمْ تَاْتِهِمْ بَيِّنَةُ مَا فِي الصُّحُفِ الْاُوْلٰى ﴿١٣٣﴾

135. Na lau kama Tungaliwaangamiza kwa adhabu kabla yake (Mtume), wangesema: Ee Mola wetu, mbona Hukutuletea Mtume tukazifuata Aya Zako kabla sisi kudhilika na kufedheheka?

وَلَوْ اَنَّاۤ اَهْلَكْنٰهُمْ بِعَذَابٍ مِّنْ قَبْلِهٖ لَقَالُوْا رَبَّنَا لَوْ لَاۤ اَرْسَلْتَ اِلَيْنَا رَسُوْلًا فَنَتَّبِعَ اٰيٰتِكَ مِنْ قَبْلِ اَنْ نَّذِلَّ وَنَخْزٰى ﴿١٣٤﴾

136. Sema: Kila mmoja anangoja, basi nanyi pia ngojeni: hivi karibuni mtajua ni nani mwenye njia iliyo sawa na ni nani aliyeongoka.

قُلْ كُلٌّ مُّتَرَبِّصٌ فَتَرَبَّصُوْا ۚ فَسَتَعْلَمُوْنَ مَنْ اَصْحٰبُ الصِّرَاطِ السَّوِيِّ وَمَنِ اهْتَدٰى ﴿١٣٥﴾ ع ۱۷

سُوْرَةُ الْاَنْبِيَآءِ مَكِّيَّةٌ وَّ هِيَ مَعَ الْبَسْمَلَةِ مِائَةٌ وَّ ثَلَاثَ عَشْرَةَ اٰيَةً وَّ سَبْعَةُ رُكُوْعَاتٍ

21. SURA AL-ANBIYAA

Imeteremshwa Makka

Ina mafungu 7 na Aya 113 pamoja na Bismillahi

JUZU 17

بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ ①

1. Kwa jina la Allah, Mwingi wa rehema, Mwingi wa ukarimu.

اِقْتَرَبَ لِلنَّاسِ حِسَابُهُمْ وَهُمْ فِيْ غَفْلَةٍ مُّعْرِضُوْنَ ②

2. Imewakaribia watu hesabu yao nao wamo katika mghafala wakikengeuka.

مَا يَاْتِيْهِمْ مِّنْ ذِكْرٍ مِّنْ رَّبِّهِمْ مُّحْدَثٍ اِلَّا اسْتَمَعُوْهُ وَهُمْ يَلْعَبُوْنَ ③

3. Hayawafikii mawaidha mapya kutoka kwa Mola wao ila huyasikia na hali wakicheza.

لَاهِيَةً قُلُوْبُهُمْ ؕ وَاَسَرُّوا النَّجْوَى ۖ الَّذِيْنَ ظَلَمُوْا ۖ هَلْ هٰذَآ اِلَّا بَشَرٌ مِّثْلُكُمْ ۚ اَفَتَاْتُوْنَ السِّحْرَ وَاَنْتُمْ تُبْصِرُوْنَ ④

4. Na mioyo yao ni misahaulifu. Na wanashauriana kwa siri wale waliodhulumu, (kisha wanasema): Huyu ni binadamu tu kama ninyi? Basi je mtapafikia mahali penye uchawi hali mnaona?

قٰلَ رَبِّيْ يَعْلَمُ الْقَوْلَ فِي السَّمَآءِ وَالْاَرْضِ ۖ وَهُوَ السَّمِيْعُ الْعَلِيْمُ ⑤

5. Alisema: Mola wangu Huyajua yaliyosemwa mbinguni na ardhini; naye ndiye Asikiaye, Ajuaye.

بَلْ قَالُوْٓا اَضْغَاثُ اَحْلَامٍ بَلِ افْتَرٰىهُ بَلْ هُوَ شَاعِرٌ ۚ فَلْيَاْتِنَا بِاٰيَةٍ كَمَآ اُرْسِلَ الْاَوَّلُوْنَ ⑥

6. Lakini wanasema: Ndoto zilizovurugika; bali ameyabuni mwenyewe, bali yu mshairi. Basi atuletee Ishara kama walivyotumwa (Mitume) wa kwanza.

Sura hii imepewa jina *Manabii* kwa kuwa imeeleza habari za kusalimishwa Manabii na kufanywa washinde. Habari za Nabii Ibrahimu ambaye ni baba wa Manabii wengi zimeelezwa ili kuwa mfano unaokaribiana zaidi na habari za Mtume *s.a.w.* Sura hii nzima ilishuka Makka.

Aya 4 - 6. Aya hizi zinaonyesha jinsi wasioamini walivyokuwa wakibabaika. Walipoona Qur'an inawavuta ingawa hawaitaki wakaiita *sihr* yaani ufasihi (Taj). Na waliposikia bishara ilizotabiri ambazo ufasihi mtupu hauwezi kuzileta, basi wakaiita, *Ndoto zilizovurugika.* Lakini tena wanaona Qur'an inazidi kutia mkazo juu ya kushindwa kwao na kushinda kwa Uislamu, hata wanaanza kufikiri haikosi kuna jambo, na kwa kujitia hamnazo wanasema, *ameyabuni mwenyewe.* Kisha wanamwita Mtume *s.a.w.* kwa jina moja lenye kukusanya namna hizo zote na wanasema yeye ni *mshairi.*

مَآ اٰمَنَتْ قَبْلَهُمْ مِّنْ قَرْيَةٍ اَهْلَكْنٰهَا ۚ اَفَهُمْ يُؤْمِنُوْنَ ۝٧

7. Haukuamini kabla yao mji wo wote Tuliouangamiza: je, wao wataamini?

وَمَآ اَرْسَلْنَا قَبْلَكَ اِلَّا رِجَالًا نُّوْحِيْٓ اِلَيْهِمْ فَسْـَٔلُوْٓا اَهْلَ الذِّكْرِ اِنْ كُنْتُمْ لَا تَعْلَمُوْنَ ۝٨

8. Na Hatukuwatuma kabla yako ila wanaume Tuliowafunulia. Basi waulizeni wenye kumbukumbu ikiwa nyinyi hamjui.

وَمَا جَعَلْنٰهُمْ جَسَدًا لَّا يَاْكُلُوْنَ الطَّعَامَ وَمَا كَانُوْا خٰلِدِيْنَ ۝٩

9. Wala hatukuwajaalia miili isiyokula chakula, wala hawakuwa wenye kukaa milele.

ثُمَّ صَدَقْنٰهُمُ الْوَعْدَ فَاَنْجَيْنٰهُمْ وَمَنْ نَّشَآءُ وَاَهْلَكْنَا الْمُسْرِفِيْنَ ۝١٠

10. Kisha Tukawasadikishia ahadi na Tukawaokoa pamoja na wale Tuliowataka na Tukawaangamiza wanaopita kiasi.

لَقَدْ اَنْزَلْنَآ اِلَيْكُمْ كِتٰبًا فِيْهِ ذِكْرُكُمْ ۭ اَفَلَا تَعْقِلُوْنَ ۝١١ ع

11. Bila shaka Tumewateremshieni Kitabu ambamo mmetajwa ndani yake ; basi je hamfahamu?

FUNGU 2

وَكَمْ قَصَمْنَا مِنْ قَرْيَةٍ كَانَتْ ظَالِمَةً وَّاَنْشَاْنَا بَعْدَهَا قَوْمًا اٰخَرِيْنَ ۝١٢

12. Na mingapi Tuliiharibu katika miji iliyokuwa ikidhulumu na Tukawaumba baadaye watu wengine?

فَلَمَّآ اَحَسُّوْا بَاْسَنَآ اِذَا هُمْ مِّنْهَا يَرْكُضُوْنَ ۝١٣ ۭ

13. Basi walipohisi adhabu Yetu, lo! wakaanza kuikimbia.

لَا تَرْكُضُوْا وَارْجِعُوْٓا اِلٰى مَآ اُتْرِفْتُمْ فِيْهِ وَمَسٰكِنِكُمْ لَعَلَّكُمْ تُسْـَٔلُوْنَ ۝١٤

14. Msikimbie, na rudini kwenye yale mliyojifurahisha nayo na kwenye maskani zenu laala ninyi mtaulizwa.

Aya 9. Aya hii inaonyesha ya kuwa hata Manabii walipewa miili yenye kula chakula na yenye kufa, na hawakuwa wawezao kukaa milele. Hivyo, ni wazi kabisa, haiwezekani kabisa Nabii Isa au Nabii ye yote kukaa mbinguni na kiwiliwili chake bila kula chakula, wala haiwezekani ya kwamba akae milele hai kiasi cha miaka 2,000.

Aya 11. *Dhikr.* Neno hili tumelifasiri "mauidha." Kadhalika lina maana ya: (1) Utukufu; (2) sifa nzuri; (3) heshima; na kadha wa kadha (Taj, Lane n.k.w.). Hivyo makafiri wanapoomba Ishara kama za Manabii wa zamani, wakitaka waangamizwe kama walivyoangamizwa waliotangulia ikiwa Uislamu ni dini ya kweli, Allah anawaambia ya kuwa amewaletea Qur'an ili iwafanye kuwa watu wakubwa wenye sifa na heshima.

15. Wakasema: Ole wetu! Hakika tulikuwa wadhalimu.

قَالُوْا يٰوَيْلَنَآ اِنَّا كُنَّا ظٰلِمِيْنَ ﴿١٥﴾

16. Na kukaendelea kulia kwao huku hata Tukawafanya waliofyekwa, wakazimika.

فَمَا زَالَتْ تِّلْكَ دَعْوٰىهُمْ حَتّٰى جَعَلْنٰهُمْ حَصِيْدًا خٰمِدِيْنَ ﴿١٦﴾

17. Na Hatukuziumba mbingu na ardhi na vilivyomo kati yao kwa mchezo.

وَمَا خَلَقْنَا السَّمَآءَ وَالْاَرْضَ وَمَا بَيْنَهُمَا لٰعِبِيْنَ ﴿١٧﴾

18. Kama Tungalitaka kufanya mchezo, hakika Tungeufanya Sisi wenyewe: kama Tungekuwa Wafanyao.

لَوْ اَرَدْنَآ اَنْ نَّتَّخِذَ لَهْوًا لَّاتَّخَذْنٰهُ مِنْ لَّدُنَّآ ۖ اِنْ كُنَّا فٰعِلِيْنَ ﴿١٨﴾

19. Bali Tunaitupa haki juu ya batili inayovunja kichwa chake na mara (batili) inatoweka; na ole wenu kwa ajili ya mnayonena!

بَلْ نَقْذِفُ بِالْحَقِّ عَلَى الْبَاطِلِ فَيَدْمَغُهٗ فَاِذَا هُوَ زَاهِقٌ ۭ وَلَكُمُ الْوَيْلُ مِمَّا تَصِفُوْنَ ﴿١٩﴾

20. Na ni Vyake vilivyomo mbinguni na ardhini; na walio mbele Yake hawajivuni kwa kumwabudu wala hawachoki.

وَلَهٗ مَنْ فِي السَّمٰوٰتِ وَالْاَرْضِ ۭ وَمَنْ عِنْدَهٗ لَا يَسْتَكْبِرُوْنَ عَنْ عِبَادَتِهٖ وَلَا يَسْتَحْسِرُوْنَ ﴿٢٠﴾

21. Wanamtukuza usiku na mchana, bila ya kusita.

يُسَبِّحُوْنَ الَّيْلَ وَالنَّهَارَ لَا يَفْتُرُوْنَ ﴿٢١﴾

22. Au wamepata waungu katika ardhi waumbao?

اَمِ اتَّخَذُوْٓا اٰلِهَةً مِّنَ الْاَرْضِ هُمْ يُنْشِرُوْنَ ﴿٢٢﴾

23. Kama humo mbinguni na ardhini kungelikuwako na miungu wengine licha ya Allah, basi zote mbingu na ardhi zingeharibika. Basi Ametakasika Allah, Mola wa Arshi, Yu mbali na yale wanayoyasifu.

لَوْ كَانَ فِيْهِمَآ اٰلِهَةٌ اِلَّا اللّٰهُ لَفَسَدَتَا ۚ فَسُبْحٰنَ اللّٰهِ رَبِّ الْعَرْشِ عَمَّا يَصِفُوْنَ ﴿٢٣﴾

24. Haulizwi Anayoyafanya lakini wao wataulizwa.

لَا يُسْـَٔلُ عَمَّا يَفْعَلُ وَهُمْ يُسْـَٔلُوْنَ ﴿٢٤﴾

25. Au je, wameshika badala Yake miungu? Sema: Leteni dalili zenu. Huu ni ukumbusho wa wale walio pamoja nami, na ukumbusho wa wale wa kabla yangu; lakini wengi wao hawajui ukweli, kwa hiyo wanapuuza.

اَمِ اتَّخَذُوْا مِنْ دُوْنِهٖٓ اٰلِهَةً ۭ قُلْ هَاتُوْا بُرْهَانَكُمْ ۚ هٰذَا ذِكْرُ مَنْ مَّعِيَ وَذِكْرُ مَنْ قَبْلِيْ ۭ بَلْ اَكْثَرُهُمْ لَا يَعْلَمُوْنَ ۙ الْحَقَّ فَهُمْ مُّعْرِضُوْنَ ﴿٢٥﴾

وَمَآ اَرْسَلْنَا مِنْ قَبْلِكَ مِنْ رَّسُوْلٍ اِلَّا نُوْحِيْٓ اِلَيْهِ اَنَّهٗ لَآ اِلٰهَ اِلَّآ اَنَا فَاعْبُدُوْنِ ﴿٢٦﴾

26. Na Hatukumtuma kabla yako Mtume ye yote ila Tulimfunulia ya kwamba hakuna aabudiwaye ila Mimi, basi Niabuduni.

وَقَالُوا اتَّخَذَ الرَّحْمٰنُ وَلَدًا سُبْحٰنَهٗ ؕ بَلْ عِبَادٌ مُّكْرَمُوْنَ ﴿٢٧﴾

27. Na wanasema: Mungu Mwenye huruma Amepanga mwana; Ametakasika (na hayo)! bali wao ni watumishi waheshimiwao.

لَا يَسْبِقُوْنَهٗ بِالْقَوْلِ وَهُمْ بِاَمْرِهٖ يَعْمَلُوْنَ ﴿٢٨﴾

28. Hawamtangulii kwa usemi, nao hufanya kwa amri Yake.

يَعْلَمُ مَا بَيْنَ اَيْدِيْهِمْ وَمَا خَلْفَهُمْ وَلَا يَشْفَعُوْنَ ۙ اِلَّا لِمَنِ ارْتَضٰى وَهُمْ مِّنْ خَشْيَتِهٖ مُشْفِقُوْنَ ﴿٢٩﴾

29. Anayajua yaliyo mbele yao na yaliyo nyuma yao, na hawamwombei (ye yote) ila yule Anayemridhia, nao kwa kumwogopa Yeye wananyenyekea.

وَمَنْ يَّقُلْ مِنْهُمْ اِنِّيْٓ اِلٰهٌ مِّنْ دُوْنِهٖ فَذٰلِكَ نَجْزِيْهِ جَهَنَّمَ ؕ كَذٰلِكَ نَجْزِي الظّٰلِمِيْنَ ﴿٣٠﴾ ع

30. Na atakayesema miongoni mwao: Hakika mimi ni mungu badala Yake, basi huyo Tutamlipa Jahanamu, hivyo ndivyo Tuwalipavyo wadhalimu.

FUNGU 3

اَوَلَمْ يَرَ الَّذِيْنَ كَفَرُوْٓا اَنَّ السَّمٰوٰتِ وَالْاَرْضَ كَانَتَا رَتْقًا فَفَتَقْنٰهُمَا ؕ وَجَعَلْنَا مِنَ الْمَآءِ كُلَّ شَيْءٍ حَيٍّ ؕ اَفَلَا يُؤْمِنُوْنَ ﴿٣١﴾

31. Je, hawakuona wale waliokufuru ya kwamba mbingu na ardhi vilikuwa vimeambatana kisha Tukaviambua; na Tukaumba kila kitu chenye uhai kutokana na maji; basi je, hawaamini?

وَجَعَلْنَا فِي الْاَرْضِ رَوَاسِيَ اَنْ تَمِيْدَ بِهِمْ ۪ وَجَعَلْنَا فِيْهَا فِجَاجًا سُبُلًا لَّعَلَّهُمْ يَهْتَدُوْنَ ﴿٣٢﴾

32. Na Tukaweka katika ardhi milima ili iwapatie chakula, na Tukaweka humo barabara zilizo panuka ili wapate kuongoka.

Aya 27. Hapa kumwita Yesu mtoto wa Mungu kunakanushwa kabisa na inaelezwa ya kuwa Manabii waliitwa "wana wa Mungu" katika Taurati kwa maana ya kuwa Watumishi wa Mungu wanaoheshimiwa, si zaidi kuliko hivyo.

Aya 31. *Tukafanya kwa maji kila kitu kilicho hai.* Jambo hili lilielezwa na Qur'an miaka 1,400, na lililokuwa halijulikani kwa watu limehakikishwa na elimu za kisasa ya kuwa maji ndiyo chanzo cha uhai. Kadhalika ufunuo wa Allah mara kwa mara umefananishwa na maji yanayoshuka ardhini, na ya kwamba kwa kupata uhai wa kiroho lazima Allah awe akishusha wahyi wake mara anapoona unahitajika.

وَجَعَلْنَا السَّمَآءَ سَقْفًا مَّحْفُوْظًا ۚ وَّهُمْ
عَنْ اٰيٰتِهَا مُعْرِضُوْنَ ﴿٣٢﴾

33. Na Tukaifanya mbingu kuwa dari iliyohifadhiwa, lakini wanazikengeuka Ishara Zake.

وَهُوَ الَّذِىْ خَلَقَ الَّيْلَ وَالنَّهَارَ وَالشَّمْسَ
وَالْقَمَرَ ؕ كُلٌّ فِىْ فَلَكٍ يَّسْبَحُوْنَ ﴿٣٣﴾

34. Na Yeye ndiye Aliyeumba usiku na mchana na jua na mwezi: vyote vinaogelea katika duara (zao).

وَمَا جَعَلْنَا لِبَشَرٍ مِّنْ قَبْلِكَ الْخُلْدَ ؕ
اَفَاْئِنْ مِّتَّ فَهُمُ الْخٰلِدُوْنَ ﴿٣٤﴾

35. Nasi Hatukumfanya mwanadamu ye yote wa kabla yako aishi milele. Basi kama ukifa wao wataishi milele?

كُلُّ نَفْسٍ ذَآئِقَةُ الْمَوْتِ ؕ
وَنَبْلُوْكُمْ بِالشَّرِّ وَالْخَيْرِ فِتْنَةً ؕ
وَاِلَيْنَا تُرْجَعُوْنَ ﴿٣٥﴾

36. Kila nafsi itaonja mauti; na Tunawajaribuni kwa shari na heri kuwa mtihani, na Kwetu mtarejeshwa.

وَاِذَا رَاٰكَ الَّذِيْنَ كَفَرُوْٓا اِنْ يَّتَّخِذُوْنَكَ
اِلَّا هُزُوًا ؕ اَهٰذَا الَّذِىْ يَذْكُرُ اٰلِهَتَكُمْ ۚ
وَهُمْ بِذِكْرِ الرَّحْمٰنِ هُمْ كٰفِرُوْنَ ﴿٣٦﴾

37. Na wanapokuona wale waliokufuru hawakufanyii cho chote ila mzaha, (wakisema): Je, huyu ndiye anayewataja waungu wenu? Na hao ndio wakataao mawaidha ya Mungu wa huruma.

خُلِقَ الْاِنْسَانُ مِنْ عَجَلٍ ؕ سَاُوْرِيْكُمْ اٰيٰتِىْ
فَلَا تَسْتَعْجِلُوْنِ ﴿٣٧﴾

38. Mwanadamu ameumbwa kwa haraka, hivi karibuni Nitawaonyesheni Ishara Zangu, kwa hiyo msinihimize kwa papara.

وَيَقُوْلُوْنَ مَتٰى هٰذَا الْوَعْدُ اِنْ كُنْتُمْ
صٰدِقِيْنَ ﴿٣٨﴾

39. Na wanasema: Ahadi hii itatokea lini kama mnasema kweli?

لَوْ يَعْلَمُ الَّذِيْنَ كَفَرُوْا حِيْنَ لَا يَكُفُّوْنَ
عَنْ وُّجُوْهِهِمُ النَّارَ وَلَا عَنْ
ظُهُوْرِهِمْ وَلَا هُمْ يُنْصَرُوْنَ ﴿٣٩﴾

40. Lau wangejua wale waliokufuru wakati ambao hawatauzuia Moto katika nyuso zao wala katika migongo yao wala hawatasaidiwa!

بَلْ تَاْتِيْهِمْ بَغْتَةً فَتَبْهَتُهُمْ فَلَا يَسْتَطِيْعُوْنَ
رَدَّهَا وَلَا هُمْ يُنْظَرُوْنَ ﴿٤٠﴾

41. Bali utawafikia kwa ghafla na utawashangaza, kisha hawataweza kuurudisha, wala hawatapewa muhula.

وَلَقَدِ اسْتُهْزِئَ بِرُسُلٍ مِّنْ قَبْلِكَ
فَحَاقَ بِالَّذِيْنَ سَخِرُوْا مِنْهُمْ مَّا كَانُوْا
بِهٖ يَسْتَهْزِءُوْنَ ﴿٤١﴾ ع ٢ ٣

42. Na bila shaka walifanyiwa dhihaka Mitume kabla yako; kwa hiyo yakawazinga wale waliofanya dhihaka miongoni mwao yale waliyokuwa wakiyafanyia dhihaka.

Aya 39. Ahadi wanayoihimiza ni ya kuwafikia Ishara ya adhabu ambayo waliiomba mara kwa mara.

Aya 42. Aya hii inatia mkazo ya kuwa kucheka kwa makafiri ni bure. Ushindi utakuwa

FUNGU 4

قُلْ مَنْ يَّكْلَؤُكُمْ بِالَّيْلِ وَالنَّهَارِ مِنَ الرَّحْمٰنِ ؕ بَلْ هُمْ عَنْ ذِكْرِ رَبِّهِمْ مُّعْرِضُوْنَ ﴿٤٣﴾

43. Sema: Nani anawalindeni usiku na mchana kwa Rahmani? Bali wao kwa kumkumbuka Mola wao wanakengeuka.

اَمْ لَهُمْ اٰلِهَةٌ تَمْنَعُهُمْ مِّنْ دُوْنِنَا ؕ لَا يَسْتَطِيْعُوْنَ نَصْرَ اَنْفُسِهِمْ وَلَا هُمْ مِّنَّا يُصْحَبُوْنَ ﴿٤٤﴾

44. Je, wanao miungu wanaowalinda badala Yetu? Hawawezi kujisaidia wenyewe wala hawataungwa mkono na yeyote dhidi yetu.

بَلْ مَتَّعْنَا هٰٓؤُلَآءِ وَاٰبَآءَهُمْ حَتّٰى طَالَ عَلَيْهِمُ الْعُمُرُ ؕ اَفَلَا يَرَوْنَ اَنَّا نَاْتِي الْاَرْضَ نَنْقُصُهَا مِنْ اَطْرَافِهَا ؕ اَفَهُمُ الْغٰلِبُوْنَ ﴿٤٥﴾

45. Bali Tuliwafaidisha hawa na baba zao mpaka umri wao ukawa mrefu kwao. Je, hawaoni ya kwamba Tunaifikia ardhi Tukiipunguza mipaka yake? Basi je, hao ni washindao?

قُلْ اِنَّمَآ اُنْذِرُكُمْ بِالْوَحْيِ ۖ وَلَا يَسْمَعُ الصُّمُّ الدُّعَآءَ اِذَا مَا يُنْذَرُوْنَ ﴿٤٦﴾

46. Sema: Mimi nawaonyeni kwa ufunuo tu. Na viziwi hawasikii mwito wanapoonywa.

وَلَئِنْ مَّسَّتْهُمْ نَفْحَةٌ مِّنْ عَذَابِ رَبِّكَ لَيَقُوْلُنَّ يٰوَيْلَنَآ اِنَّا كُنَّا ظٰلِمِيْنَ ﴿٤٧﴾

47. Na kama ingaliwagusa dhoruba moja ya adhabu ya Mola wako, bila shaka wangalisema: Ole wetu, hakika tulikuwa wadhalimu!

وَنَضَعُ الْمَوَازِيْنَ الْقِسْطَ لِيَوْمِ الْقِيٰمَةِ فَلَا تُظْلَمُ نَفْسٌ شَيْـًٔا ؕ وَاِنْ كَانَ مِثْقَالَ حَبَّةٍ مِّنْ خَرْدَلٍ اَتَيْنَا بِهَا ؕ وَكَفٰى بِنَا حٰسِبِيْنَ ﴿٤٨﴾

48. Nasi Tutaweka mizani ya uadilifu siku ya Kiyama, na nafsi ye yote haitadhulumiwa hata kidogo; na kama kukiwa na uzito wa chembe ya hardali Tutaileta; Nasi Twatosha kuwa Wanaohesabu.

وَلَقَدْ اٰتَيْنَا مُوْسٰى وَهٰرُوْنَ الْفُرْقَانَ وَضِيَآءً وَّ ذِكْرًا لِّلْمُتَّقِيْنَ ﴿٤٩﴾ۙ

49. Na kwa yakini Tuliwapa Musa na Harun Kipambanuzi na anga na mawaidha kwa wacha-Mungu.

الَّذِيْنَ يَخْشَوْنَ رَبَّهُمْ بِالْغَيْبِ وَهُمْ مِّنَ السَّاعَةِ مُشْفِقُوْنَ ﴿٥٠﴾

50. Ambao wanamwogopa Mola wao hata faraghani na pia huiogopa saa ile.

---

upande wenye haki tu, na Mtume na waaminio ndio watakaoshinda, na adhabu itakuwa kwa makafiri.

Aya 49. *Furqaan* "Kipambanuzi" ambacho walipewa Musa na Harun ni kuwa walimshinda adui yao aliyekuwa mfalme mwenye nguvu sana. Aya 51 inaonyesha ya kwamba maadui wa Mtume *s.a.w.* watashindwa kama vile walivyoshindwa maadui wa Nabii Musa.

51. Na haya ni mawaidha yaliyobarikiwa Tuliyoyateremsha: je, ninyi mtayakataa?

وَهٰذَا ذِكْرٌ مُّبٰرَكٌ اَنْزَلْنٰهُ ؕ اَفَاَنْتُمْ لَهٗ مُنْكِرُوْنَ ﴿٥١﴾ ع ع ٩ ٤ ٤

FUNGU 5

52. Na hakika Tulimpa Ibrahimu mwongozo wake zamani na Tulikuwa Tukimjua.

وَلَقَدْ اٰتَيْنَاۤ اِبْرٰهِيْمَ رُشْدَهٗ مِنْ قَبْلُ وَكُنَّا بِهٖ عٰلِمِيْنَ ﴿٥٢﴾ ج

53. Alipomwambia baba yake na watu wake: Ni nini masanamu haya mnayoyategemea?

اِذْ قَالَ لِاَبِيْهِ وَقَوْمِهٖ مَا هٰذِهِ التَّمَاثِيْلُ الَّتِيْۤ اَنْتُمْ لَهَا عٰكِفُوْنَ ﴿٥٣﴾

54. Wakasema, Tuliwakuta baba zetu wakiyaabudu.

قَالُوْا وَجَدْنَاۤ اٰبَآءَنَا لَهَا عٰبِدِيْنَ ﴿٥٤﴾

55. Akasema: Bila shaka ninyi na baba zenu mlikuwa katika upotevu dhahiri.

قَالَ لَقَدْ كُنْتُمْ اَنْتُمْ وَاٰبَآؤُكُمْ فِيْ ضَلٰلٍ مُّبِيْنٍ ﴿٥٥﴾

56. Wakasema: Je, umetufikia kwa haki au u miongoni mwa wachezaji?

قَالُوْۤا اَجِئْتَنَا بِالْحَقِّ اَمْ اَنْتَ مِنَ اللّٰعِبِيْنَ ﴿٥٦﴾

57. Akasema: Siyo! Mola wenu ndiye Mola wa mbingu na ardhi Ambaye Aliziumba, nami juu ya hayo ni miongoni mwa washuhudiao.

قَالَ بَلْ رَّبُّكُمْ رَبُّ السَّمٰوٰتِ وَالْاَرْضِ الَّذِيْ فَطَرَهُنَّ ۖ وَاَنَا عَلٰى ذٰلِكُمْ مِّنَ الشّٰهِدِيْنَ ﴿٥٧﴾

58. Na haki ya Mungu! kwa yakini nitayafanya vibaya masanamu yenu baada ya kugeuka mkirudi.

وَتَاللّٰهِ لَاَكِيْدَنَّ اَصْنَامَكُمْ بَعْدَ اَنْ تُوَلُّوْا مُدْبِرِيْنَ ﴿٥٨﴾

59. Basi akayavunja vipande vipande isipokuwa kubwa lao, ili wao walirudie.

فَجَعَلَهُمْ جُذٰذًا اِلَّا كَبِيْرًا لَّهُمْ لَعَلَّهُمْ اِلَيْهِ يَرْجِعُوْنَ ﴿٥٩﴾

60. Wakasema: Nani amefanya hivi kwa miungu wetu? Hakika huyo yu miongoni mwa wadhalimu!

قَالُوْا مَنْ فَعَلَ هٰذَا بِاٰلِهَتِنَاۤ اِنَّهٗ لَمِنَ الظّٰلِمِيْنَ ﴿٦٠﴾

61. Wakasema: tulimsikia kijana mmoja akiwasema, anaitwa Ibrahimu.

قَالُوْا سَمِعْنَا فَتًى يَّذْكُرُهُمْ يُقَالُ لَهٗۤ اِبْرٰهِيْمُ ؕ ﴿٦١﴾

Aya 52. Habari za Nabii Ibrahimu zimetajwa katika sehemu mbalimbali za Qur'an kama hivi: Sura 2:125-134, 136, 141, 259, 261; 3:66-69, 83; 4:126; 6:75-83; 9:114; 11:70-77; 12:7; 14:36-42; 15:52-61; 16:121-124; 19:42-50; 21:52-73; 22:27; 26:70-88; 29:17, 18, 26-28; 37:84-114; 38:46, 48; 43:27-29; 51:25-33; 57:27; 60:4.

قَالُوْا فَاْتُوْا بِهٖ عَلٰٓى اَعْيُنِ النَّاسِ لَعَلَّهُمْ يَشْهَدُوْنَ ﴿٦١﴾

62. Wakasema: Basi mleteni mbele ya macho ya watu, huenda watashuhudia.

قَالُوْٓا ءَاَنْتَ فَعَلْتَ هٰذَا بِاٰلِهَتِنَا يٰٓاِبْرٰهِيْمُ ﴿٦٢﴾

63. Wakasema: Je wewe umewafanya hivi miungu wetu, ee Ibrahimu?

قَالَ بَلْ فَعَلَهٗ ۖ كَبِيْرُهُمْ هٰذَا فَسْـَٔلُوْهُمْ اِنْ كَانُوْا يَنْطِقُوْنَ ﴿٦٣﴾

64. Akajibu: Bali amefanya,mkubwa wao huyu, basi waulizeni kama wanaweza kunena.

فَرَجَعُوْٓا اِلٰٓى اَنْفُسِهِمْ فَقَالُوْٓا اِنَّكُمْ اَنْتُمُ الظّٰلِمُوْنَ ﴿٦٤﴾

65. Basi wakajirudi nafsi zao na wakasema: Hakika ninyi mlikuwa wadhalimu.

ثُمَّ نُكِسُوْا عَلٰى رُءُوْسِهِمْ ۚ لَقَدْ عَلِمْتَ مَا هٰٓؤُلَآءِ يَنْطِقُوْنَ ﴿٦٥﴾

66. Kisha wakainamishwa vichwa vyao (kwa kukosa majibu), (wakasema): Hakika umekwisha jua ya kwamba hawa hawasemi.

قَالَ اَفَتَعْبُدُوْنَ مِنْ دُوْنِ اللّٰهِ مَا لَا يَنْفَعُكُمْ شَيْـًٔا وَّلَا يَضُرُّكُمْ ﴿٦٦﴾

67. Akasema: Je, mnaabudu badala ya Allah yasiyowafaeni cho chote wala kuwadhuruni?

اُفٍّ لَّكُمْ وَلِمَا تَعْبُدُوْنَ مِنْ دُوْنِ اللّٰهِ ۭ اَفَلَا تَعْقِلُوْنَ ﴿٦٧﴾

68. Kefule kwenu na kwa hivyo mnavyoviabudu kinyume cha Allah; je, hamtumii akili?

Aya 64. Baadhi ya wafasiri wanakwepa tafsiri ya neno kwa neno ya aya hii wakihofia kwamba hii itamfanya Ibrahimu aonekane kuwa ni muongo. Ni dhahiri kwamba zile sanamu ndogo ndogo hazikuvunjwa na lile sanamu kubwa bali alikuwa Ibrahimu aliyefanya hivyo. Kwa hiyo kuyanasibisha kwa Ibrahimu maneno "huyu hapa ndiye mkubwa wao", kutakuwa sawasawa kabisa na kunasibisha uwongo ulio wazi kwa Ibrahimu. Lakini ni lazima izingatiwe kwamba haikuwa kauli potofu bali ulikuwa mtindo madhubuti wa kutoa hoja. Mara nyingine jambo linakuwa bayana sana kwa mtu ye yote kuliamini, na kauli ya kuelezea hivyo kamwe haieleweki kuwa ni jaribio la kuwapoteza wengine kwa makusudi bali inahesabiwa kuwa ni uwekaji bayana wa upuuzi asilia wa hali fulani. Tunaamini kwamba Ibrahimu aliitoa kauli ile bila ya kuwa na walau nia ndogo kabisa ya kuwapoteza bali ilikuwa ni njia tu ya kutoa hoja madhubuti dhidi wa uwongo wa imani yao. Na hivyo ndivyo hasa walivyoichukulia kauli hiyo. Baada ya kumsikiliza Ibrahimu hakuna ye yote miongoni mwao aliyejibu kwa kumwita Ibrahimu kuwa ni mwongo. Bali kwa mujibu wa Qur'an Tukufu walilazimika kutafakari na hatimaye wakautambua upuuzi wa imani yao. Jambo hili linawekwa wazi zaidi katika aya zinazofuatia. (tazama aya ya 65 hadi 68). Tena ni lazima ikumbukwe kwamba kabla ya tukio hili Ibrahimu mwenyewe alitaja hadharani nia yake ya kuyavunja masanamu yao (tazama aya ya 58).

Aya 66. *Wakainamishwa vichwa vyao,* yaani walifedheheka kuona waungu wao hawakuweza kujisaidia.

قَالُوْا حَرِّقُوْهُ وَانْصُرُوْٓا اٰلِهَتَكُمْ اِنْ كُنْتُمْ فٰعِلِيْنَ ﴿٦٩﴾

69. Wakasema: Muunguzeni na mwasaidie miungu wenu, ikiwa ninyi ni watendao.

قُلْنَا يٰنَارُ كُوْنِيْ بَرْدًا وَّسَلٰمًا عَلٰٓى اِبْرٰهِيْمَ ﴿٧٠﴾

70. Tukasema: Ewe Moto, uwe baridi na salama kwa ajili ya Ibrahimu.

وَاَرَادُوْا بِهٖ كَيْدًا فَجَعَلْنٰهُمُ الْاَخْسَرِيْنَ ﴿٧١﴾

71. Na wakamtakia ubaya, lakini Tukawafanya kuwa wapatao hasara kuu.

وَنَجَّيْنٰهُ وَلُوْطًا اِلَى الْاَرْضِ الَّتِيْ بٰرَكْنَا فِيْهَا لِلْعٰلَمِيْنَ ﴿٧٢﴾

72. Na Tulimwokoa yeye na Luti kwenye ardhi Tuliyoibarikia kwa ajili ya walimwengu.

وَوَهَبْنَا لَهٗٓ اِسْحٰقَ ؕ وَيَعْقُوْبَ نَافِلَةً ؕ وَكُلًّا جَعَلْنَا صٰلِحِيْنَ ﴿٧٣﴾

73. Naye Tukampa Isihaka, na Yakubu mjukuu; na wote Tukawafanya kuwa wema.

وَجَعَلْنٰهُمْ اَئِمَّةً يَّهْدُوْنَ بِاَمْرِنَا وَاَوْحَيْنَآ اِلَيْهِمْ فِعْلَ الْخَيْرٰتِ وَاِقَامَ الصَّلٰوةِ وَاِيْتَآءَ الزَّكٰوةِ ۚ وَكَانُوْا لَنَا عٰبِدِيْنَ ﴿٧٤﴾

74. Na Tukawajaalia kuwa Maimamu wanaoongoza kwa amri Yetu, na Tukawafunulia kuzifanya heri na kusimamisha Sala na kutoa Zaka; nao walikuwa wakituabudu.

وَلُوْطًا اٰتَيْنٰهُ حُكْمًا وَّعِلْمًا وَّنَجَّيْنٰهُ مِنَ الْقَرْيَةِ الَّتِيْ كَانَتْ تَّعْمَلُ الْخَبٰٓئِثَ ؕ اِنَّهُمْ كَانُوْا قَوْمَ سَوْءٍ فٰسِقِيْنَ ﴿٧٥﴾

75. Na Luti Tukampa hukumu na elimu na Tukamwokoa katika mji uliokuwa ukifanya maovu; bila shaka wao walikuwa watu wabaya, wavunjao amri.

وَاَدْخَلْنٰهُ فِيْ رَحْمَتِنَا ؕ اِنَّهٗ مِنَ الصّٰلِحِيْنَ ﴿٧٦﴾

76. Na Tukamwingiza katika rehema Zetu; hakika yeye alikuwa miongoni mwa wafanyao mema.

FUNGU 6

وَنُوْحًا اِذْ نَادٰى مِنْ قَبْلُ فَاسْتَجَبْنَا لَهٗ فَنَجَّيْنٰهُ وَاَهْلَهٗ مِنَ الْكَرْبِ الْعَظِيْمِ ﴿٧٧﴾

77. Na Nuhu alipoita zamani, nasi Tukamwitikia, na Tukamwokoa yeye na watu wake katika msiba mkubwa.

وَنَصَرْنٰهُ مِنَ الْقَوْمِ الَّذِيْنَ كَذَّبُوْا بِاٰيٰتِنَا ؕ اِنَّهُمْ كَانُوْا قَوْمَ سَوْءٍ فَاَغْرَقْنٰهُمْ اَجْمَعِيْنَ ﴿٧٨﴾

78. Na Tukamsaidia yeye juu ya watu waliozikadhibisha Aya Zetu; hakika wao walikuwa watu wabaya, basi Tukawagharikisha wote.

79. Na Daudi na Suleimani, walipokata hukumu juu ya shamba, walipolisha humo mbuzi wa watu usiku, nasi kwa hukumu yao Tulikuwa Mashahidi.

وَدَاوٗدَ وَسُلَيْمٰنَ اِذْ يَحْكُمٰنِ فِي الْحَرْثِ اِذْ نَفَشَتْ فِيْهِ غَنَمُ الْقَوْمِ ۚ وَكُنَّا لِحُكْمِهِمْ شٰهِدِيْنَ ﴿٧٩﴾

80. Hivyo Tukamfahamisha Suleimani; na kila mmoja Tukampa hukumu na elimu; na Tukaitiisha, pamoja na Daudi, milima, ikitukuza na ndege pia; na Sisi Tulikuwa Wafanyao.

فَفَهَّمْنٰهَا سُلَيْمٰنَ ۚ وَكُلًّا اٰتَيْنَا حُكْمًا وَّعِلْمًا ۡ وَّسَخَّرْنَا مَعَ دَاوٗدَ الْجِبَالَ يُسَبِّحْنَ وَالطَّيْرَ ؕ وَكُنَّا فٰعِلِيْنَ ﴿٨٠﴾

81. Na Tukamfundisha matengenezo ya mavazi kwa ajili yenu ili yawahifadhini katika mapigano yenu; je, ninyi mtakuwa wanaoshukuru?

وَعَلَّمْنٰهُ صَنْعَةَ لَبُوْسٍ لَّكُمْ لِتُحْصِنَكُمْ مِّنْۢ بَاْسِكُمْ ۚ فَهَلْ اَنْتُمْ شٰكِرُوْنَ ﴿٨١﴾

82. Na kwa Suleimani (Tukautiisha) upepo wa nguvu uendao kwa amri yake kwenye ardhi ambayo Tumeibarikia, nasi ndio Tunaokijua kila kitu.

وَلِسُلَيْمٰنَ الرِّيْحَ عَاصِفَةً تَجْرِيْ بِاَمْرِهٖۤ اِلَى الْاَرْضِ الَّتِيْ بٰرَكْنَا فِيْهَا ؕ وَكُنَّا بِكُلِّ شَيْءٍ عٰلِمِيْنَ ﴿٨٢﴾

83. Na katika mashetani (walikuwapo) wenye kumpigia mbizi na wakimfanyia vitendo zaidi ya hivyo: nasi Tulikuwa Walinzi wao.

وَمِنَ الشَّيٰطِيْنِ مَنْ يَّغُوْصُوْنَ لَهٗ وَيَعْمَلُوْنَ عَمَلًا دُوْنَ ذٰلِكَ ۚ وَكُنَّا لَهُمْ حٰفِظِيْنَ ﴿٨٣﴾ۙ

84. Na Ayubu, alipomwita Mola wake ya kwamba imenigusa dhara, nawe ndiwe Unayerehemu zaidi kuliko wanaorehemu.

وَاَيُّوْبَ اِذْ نَادٰى رَبَّهٗۤ اَنِّيْ مَسَّنِيَ الضُّرُّ وَاَنْتَ اَرْحَمُ الرّٰحِمِيْنَ ﴿٨٤﴾ۚ

85. Basi Tukamkubalia wito wake na Tukamwondolea dhara aliyokuwa nayo, na Tukampa ahali zake na mfano wao pamoja nao: ni rehema kutoka Kwetu, na ukumbusho kwa wafanyao ibada.

فَاسْتَجَبْنَا لَهٗ فَكَشَفْنَا مَا بِهٖ مِنْ ضُرٍّ ۖ وَّاٰتَيْنٰهُ اَهْلَهٗ وَمِثْلَهُمْ مَّعَهُمْ رَحْمَةً مِّنْ عِنْدِنَا وَذِكْرٰى لِلْعٰبِدِيْنَ ﴿٨٥﴾

86. Na Ismaili, na Idrisa, na Dhul-Kifli - wote walikuwa miongoni mwa wanaosubiri.

وَاِسْمٰعِيْلَ وَاِدْرِيْسَ وَذَا الْكِفْلِ ؕ كُلٌّ مِّنَ الصّٰبِرِيْنَ ﴿٨٦﴾ۚ

Aya 86. *Dhul-Kifl.* Wanazuoni wanahitilafiana Nabii huyu Dhul-Kifl ni nani, na wanampambanisha na Nabii Zakaria, au Elia au Yashua. Kadhalika inasimuliwa ya kwamba Waarabu wanamwita Nabii Ezekiel kwa jina la Kifl. Yumkini yeye ndiye Dhul-Kifl.

وَاَدْخَلْنٰهُمْ فِیْ رَحْمَتِنَا ؕ اِنَّهُمْ مِّنَ الصّٰلِحِیْنَ ﴿۸۶﴾

87. Na Tukawaingiza katika rehema Zetu; hakika wao walikuwa katika watu wema.

وَذَا النُّوْنِ اِذْ ذَّهَبَ مُغَاضِبًا فَظَنَّ اَنْ لَّنْ نَّقْدِرَ عَلَیْهِ فَنَادٰی فِی الظُّلُمٰتِ اَنْ لَّاۤ اِلٰهَ اِلَّاۤ اَنْتَ سُبْحٰنَكَ ۖ اِنِّیْ كُنْتُ مِنَ الظّٰلِمِیْنَ ﴿۸۷﴾

88. Na kumbukeni alipoondoka Dhun-Nuni hali amechukia. Na akadhani ya kwamba Hatutamdhikisha. Kisha kutoka katika giza nene akanadi: Kwamba hapana aabudiwaye isipokuwa Wewe. U Mtakatifu. Hakika mimi nilikuwa miongoni mwa wadhalimu.

فَاسْتَجَبْنَا لَهٗ ۙ وَنَجَّیْنٰهُ مِنَ الْغَمِّ ؕ وَكَذٰلِكَ نُنْجِی الْمُؤْمِنِیْنَ ﴿۸۸﴾

89. Basi Tukampokelea na Tukamwokoa katika huzuni, na hivyo ndivyo Tuwaokoavyo waaminio.

وَزَكَرِیَّاۤ اِذْ نَادٰی رَبَّهٗ رَبِّ لَا تَذَرْنِیْ فَرْدًا وَّاَنْتَ خَیْرُ الْوٰرِثِیْنَ ﴿۸۹﴾

90. Na Zakaria alipomwita Mola wake, Mola wangu! Usiniache peke yangu; na Wewe ndiwe Mbora wa wanaorithi.

فَاسْتَجَبْنَا لَهٗ ۟ وَوَهَبْنَا لَهٗ یَحْیٰی وَاَصْلَحْنَا لَهٗ زَوْجَهٗ ؕ اِنَّهُمْ كَانُوْا یُسٰرِعُوْنَ فِی الْخَیْرٰتِ وَیَدْعُوْنَنَا رَغَبًا وَّرَهَبًا ؕ وَكَانُوْا لَنَا خٰشِعِیْنَ ﴿۹۰﴾

91. Basi Tukampokelea na Tukampa Yahya na Tukamponyeshea mkewe; bila shaka wao walikuwa wepesi kufanya wema, na wakatuomba kwa shauku na hofu; nao walikuwa wakitunyenyekea.

وَالَّتِیْۤ اَحْصَنَتْ فَرْجَهَا فَنَفَخْنَا فِیْهَا مِنْ رُّوْحِنَا وَجَعَلْنٰهَا وَابْنَهَاۤ اٰیَةً لِّلْعٰلَمِیْنَ ﴿۹۱﴾

92. Na mkumbukeni yule mwanamke aliyelinda tupu yake na Tukampulizia roho yetu na Tukamfanya yeye na mwanawe Ishara kwa walimwengu.

اِنَّ هٰذِهٖۤ اُمَّتُكُمْ اُمَّةً وَّاحِدَةً ۖ وَّاَنَا رَبُّكُمْ فَاعْبُدُوْنِ ﴿۹۲﴾

93. Kwa yakini hilo ni kundi lenu, lililo kundi moja tu, na Mimi ni Mola wenu, kwa hiyo Niabuduni.

وَتَقَطَّعُوْۤا اَمْرَهُمْ بَیْنَهُمْ ؕ كُلٌّ اِلَیْنَا رٰجِعُوْنَ ﴿۹۳﴾ ع

94. Nao wakajikatia dini yao vipande vipande: wote ni warudiao Kwetu.

Aya 88. *Dhun-Nuun* ni Nabii Yunus. Kwa jina la Yunus ametajwa katika Sura 6:87; 10:99 na 37:140. Neno *Dhun-Nuun* maana yake ni *Mwenye samaki.* Katika sura 68:49 Nabii Yunus ameitwa kwa jina, *Saahibul Huut* yaani *Mwenzi wa samaki.*

Nilikuwa miongoni mwa wadhalimu. Neno *dhulm* lililotumiwa katika Kiarabu pia lina maana ya hasara (Taj), na hivyo hapa maneno hayo yanaweza kusomwa hivi: *Nilikuwa miongoni mwa wenye hasara.*

FUNGU 7

فَمَنْ يَّعْمَلْ مِنَ الصّٰلِحٰتِ وَهُوَ مُؤْمِنٌ فَلَا كُفْرَانَ لِسَعْيِهٖ ۚ وَاِنَّا لَهٗ كٰتِبُوْنَ ﴿٩٤﴾

95. Basi ye yote atakayefanya vitendo vizuri hali yu mwumini, basi haitakataliwa juhudi yake na bila shaka Sisi ni wenye kuiandika kwa ajili yake.

وَحَرٰمٌ عَلٰى قَرْيَةٍ اَهْلَكْنٰهَآ اَنَّهُمْ لَا يَرْجِعُوْنَ ﴿٩٥﴾

96. Na ni haramu kwa mji Tulioungamiza ya kwamba wao hawatarejea.

حَتّٰٓى اِذَا فُتِحَتْ يَاْجُوْجُ وَمَاْجُوْجُ وَهُمْ مِّنْ كُلِّ حَدَبٍ يَّنْسِلُوْنَ ﴿٩٦﴾

97. Hata atakapofunguliwa Yajuja na Majuja, nao toka kila mahali pa juu watakuja mbiombio.

وَاقْتَرَبَ الْوَعْدُ الْحَقُّ فَاِذَا هِيَ شَاخِصَةٌ اَبْصَارُ الَّذِيْنَ كَفَرُوْا ؕ يٰوَيْلَنَا قَدْ كُنَّا فِيْ غَفْلَةٍ مِّنْ هٰذَا بَلْ كُنَّا ظٰلِمِيْنَ ﴿٩٧﴾

98. Na itakaribia ahadi ya haki, ndipo yatakodoka macho ya wale waliokufuru (wakisema): Ole wetu! bila shaka Tulikuwa katika mghafiliko na (jambo) hili, bali tulikuwa wadhalimu.

اِنَّكُمْ وَمَا تَعْبُدُوْنَ مِنْ دُوْنِ اللّٰهِ حَصَبُ جَهَنَّمَ ؕ اَنْتُمْ لَهَا وٰرِدُوْنَ ﴿٩٨﴾

99. Hakika ninyi na wale mnaowaabudu kinyume cha Allah ni kuni za Jahanamu; mtaifikia.

لَوْ كَانَ هٰٓؤُلَآءِ اٰلِهَةً مَّا وَرَدُوْهَا ؕ وَكُلٌّ فِيْهَا خٰلِدُوْنَ ﴿٩٩﴾

100. Lau kama hawa wangalikuwa miungu wasingeifikia na wote humo watakaa.

لَهُمْ فِيْهَا زَفِيْرٌ وَّهُمْ فِيْهَا لَا يَسْمَعُوْنَ ﴿١٠٠﴾

101. Wao humo watapiga mayowe nao humo hawatasikia.

اِنَّ الَّذِيْنَ سَبَقَتْ لَهُمْ مِّنَّا الْحُسْنٰٓى ۙ اُولٰٓئِكَ عَنْهَا مُبْعَدُوْنَ ﴿١٠١﴾

102. Hakika hao ambao wema wetu ulitangulia kufika kwao, hao ndio watakaowekwa mbali nayo.

Aya 96. Aya hii inaonyesha ya kwamba wanaokufa hawarudi tena duniani. Na ya 97 inaonyesha ya kuwa hata *Yaajuuj* na *Maajuuj* (Gog na Magog), juu ya kufanikiwa kwao katika mambo ya kidunia, hawataweza kuwarejesha waliokufa. Kanuni hii ya Allah ni maarufu kabisa.

Aya 97. Aya hii inaonyesha ya kwamba wakati utafika *Yaajuuj* na *Maajuuj* watapoenea na kushinda kila mahali duniani. *Kuondoka upesi katika kila mahali pa juu* mradi wake ni kuwa watashika kila mahali patukufu na penye faida.

Aya 102. Aya hii inakanusha maneno ya Wakatoliki yanayosema kuwa hata watu wema kwanza watatiwa katika adhabu ya pagatori kabla ya kupelekwa Peponi. Qur'an inasema, watu wema watakuwa mbali kabisa na Jahanamu hata hawatasikia sauti ndogo ya ngurumo zake.

لَا يَسْمَعُوْنَ حَسِيْسَهَا ۚ وَهُمْ فِيْ مَا
اشْتَهَتْ اَنْفُسُهُمْ خٰلِدُوْنَ ﴿١٠٣﴾

103. Hawatausikia mvumo wake, nao watakaa katika yale zinayoyatamani nafsi zao.

لَا يَحْزُنُهُمُ الْفَزَعُ الْاَكْبَرُ وَتَتَلَقّٰىهُمُ
الْمَلٰٓئِكَةُ ؕ هٰذَا يَوْمُكُمُ الَّذِيْ كُنْتُمْ
تُوْعَدُوْنَ ﴿١٠٤﴾

104. Hayatawahuzunisha mahangaiko makubwa, na Malaika watawapokea: hiyo ndiyo siku yenu mliyokuwa mkiahidiwa.

يَوْمَ نَطْوِي السَّمَآءَ كَطَيِّ السِّجِلِّ
لِلْكُتُبِ ؕ كَمَا بَدَاْنَآ اَوَّلَ خَلْقٍ نُّعِيْدُهٗ ؕ
وَعْدًا عَلَيْنَا ؕ اِنَّا كُنَّا فٰعِلِيْنَ ﴿١٠٥﴾

105. Siku Tutakayoikunja mbingu kama mkunjo wa karatasi za maandiko: kama Tulivyoanza umbo la awali Tutalirudisha tena; ni ahadi iliyo juu Yetu; bila shaka Sisi ni Wafanyao.

وَلَقَدْ كَتَبْنَا فِي الزَّبُوْرِ مِنْۢ بَعْدِ الذِّكْرِ اَنَّ
الْاَرْضَ يَرِثُهَا عِبَادِيَ الصّٰلِحُوْنَ ﴿١٠٦﴾
اِنَّ فِيْ هٰذَا لَبَلٰغًا لِّقَوْمٍ عٰبِدِيْنَ ﴿١٠٧﴾

106. Na Tulikwisha andika katika Zaburi ya Daudi baada ya ukumbusho kwamba watumishi Wangu wema ndio watakaoirithi ardhi hii.

107. Hakika katika hayo umo ujumbe kwa watu wafanyao ibada.

Aya 106. *Tuliandika katika Zaburi.* Aya hii inawakumbusha Waislamu bishara tukufu iliyomo katika Zaburi 37:29, inayosema; "Wenye haki watairithi nchi, na kuikaa milele." Bishara hii ya Biblia ilitimia katika siku za Seyidna Umar, Waislamu walipoitawala nchi ya Falastini (Palestine) na ikathibitika ya kwamba Waislamu ndio "wenye haki" walioahidiwa nchi hiyo.

Kwa hakika wazao wa Nabii Ibrahimu walipewa ahadi ya kukaa katika nchi ya Falastin, na kutahiri kulikuwa alama ya ahadi ile. Katika mwanzo 17:23 mmeandikwa ya kwamba Ismaili alitahiri alipokuwa mwenye umri wa miaka 13. Lakini ahadi ya kukaa nchi ya Kanaan inapatikana kwa ajili ya Isihaka tu; na Ismaili hakushirikishwa humo, ijapokuwa alibarikiwa sana na Mungu (Mwanzo 17:20). Wana wa Israeli walipoendelea katika ukaidi wao na kuwaudhi Manabii wa Allah, walionywa na Nabii Daud ya kwamba wale tu watairithi nchi ya Kanaan ambao ni wachaji na wenye haki.

Aya 107. *Ujumbe kwa watu wafanyao ibada.* Qur'an ilipoteremka, Waislamu walikumbushwa ya kwamba wao ndio wanaostahili kutawala nchi ya Kanaan. Waislamu walipokea ujumbe huu, na wakati ulipowadia waliitimiza bishara hii kwa kuingia nchi ya Falastini. Wanaosema ya kwamba Waislamu walikuwa wahuni na wakashinda nchi ile pasipo haki na wakumbuke ya kwamba wao wanakadhibisha Qur'an na Biblia ambavyo vinawasifu Waislamu kuwa "Wafanyao ibada" na "Wenye haki."

Sawa na bishara ya Qur'an iliyomo katika sura 17:105, Mayahudi wameletwa katika Falastini, lakini hawatadumu humo. Wenye haki watarithi tena ardhi ile na imani ya waaminio itaongezeka. Padre Dale ameandika ya kwamba Mtume *s.a.w.* hakufunuliwa bishara hii na Allah, bali alikopa maneno hayo. Labda sasa amekwisha jua waziwazi hakika ilivyo.

وَمَآ اَرۡسَلۡنٰكَ اِلَّا رَحۡمَةً لِّلۡعٰلَمِيۡنَ ﴿۱۰۸﴾

108. Nasi Hatukukutuma ila uwe rehema kwa walimwengu.

قُلۡ اِنَّمَا يُوۡحٰٓى اِلَىَّ اَنَّمَآ اِلٰهُكُمۡ اِلٰهٌ وَّاحِدٌ‌ ۚ فَهَلۡ اَنۡتُمۡ مُّسۡلِمُوۡنَ ﴿۱۰۹﴾

109. Sema: Sikufunuliwa ila kwamba Mungu wenu ni Mungu Mmoja tu; je, hamtasilimu?

فَاِنۡ تَوَلَّوۡا فَقُلۡ اٰذَنۡتُكُمۡ عَلٰى سَوَآءٍ‌ ؕ وَاِنۡ اَدۡرِىۡۤ اَقَرِيۡبٌ اَمۡ بَعِيۡدٌ مَّا تُوۡعَدُوۡنَ ﴿۱۱۰﴾

110. Na kama wakigeuka, basi sema: Nimewatangazieni sawasawa, wala sijui yako karibu au mbali yale mliyoahidiwa.

اِنَّهٗ يَعۡلَمُ الۡجَهۡرَ مِنَ الۡقَوۡلِ وَيَعۡلَمُ مَا تَكۡتُمُوۡنَ ﴿۱۱۱﴾

111. Hakika Yeye Anajua kauli iliyo dhahiri na Anajua mnayoyaficha.

وَاِنۡ اَدۡرِىۡ لَعَلَّهٗ فِتۡنَةٌ لَّكُمۡ وَمَتَاعٌ اِلٰى حِيۡنٍ ﴿۱۱۲﴾

112. Wala sijui kama hii ni fitina kwenu na starehe mpaka muda kidogo.

قٰلَ رَبِّ احۡكُمۡ بِالۡحَقِّ‌ ؕ وَرَبُّنَا الرَّحۡمٰنُ الۡمُسۡتَعَانُ عَلٰى مَا تَصِفُوۡنَ ﴿۱۱۳﴾ ع

113. Akasema: Mola wangu, Uhukumu kwa haki; na Mola wetu ndiye mwenye rehema, Aombwaye msaada juu ya hayo mnayoyasema.

Aya 108. Aya hii inahakikisha ukubwa wa Mtume *s.a.w.* juu ya Manabii wote. Wao kila mmoja alitumwa kwa watu au makabila maalumu, lakini Mtume *s.a.w.* ametumwa kuwa rehema kwa dunia nzima. Mafundisho ya Qur'an yamejihakikisha kuwa rehema kwa ajili ya dunia. Yaliwainua Waarabu waliokuwa gizani yakawafanya watukufu duniani. Na zaidi ya hayo, mafundisho ya Qur'an yamekuwa rehema siku zote yanapofuatwa, hata tunaona sasa baadhi ya kanuni za Kiislamu zinaanza kuchukuliwa na watu wa Magharibi hata na Mabaniani ili zipate kuwafaa na kuwaletea raha.

سُوْرَةُ الْحَجِّ مَدَنِيَّةٌ وَّ هِيَ مَعَ الْبَسْمَلَةِ تِسْعٌ وَّ سَبْعُوْنَ اٰيَةً وَّ عَشَرَةُ رُكُوْعَاتٍ

22. SURA AL-HAJJ

Imeteremshwa Madina

Ina mafungu 10 na Aya 79 pamoja na Bismillahi

بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ ①

1. Kwa jina la Allah, Mwingi wa rehema, Mwingi wa ukarimu.

يٰۤاَيُّهَا النَّاسُ اتَّقُوْا رَبَّكُمْ ۚ اِنَّ زَلْزَلَةَ السَّاعَةِ شَيْءٌ عَظِيْمٌ ②

2. Enyi watu! Mcheni Mola wenu; hakika tetemeko la saa ile ni jambo kubwa.

يَوْمَ تَرَوْنَهَا تَذْهَلُ كُلُّ مُرْضِعَةٍ عَمَّاۤ اَرْضَعَتْ وَتَضَعُ كُلُّ ذَاتِ حَمْلٍ حَمْلَهَا وَتَرَى النَّاسَ سُكٰرٰى وَمَا هُمْ بِسُكٰرٰى وَلٰكِنَّ عَذَابَ اللّٰهِ شَدِيْدٌ ③

3. Siku mtakapoliona, kila mwanamke anyonyeshaye atamsahau amnyonyeshaye, na kila mwenye mimba ataiharibu mimba yake, na utawaona watu wamelewa, kumbe hawakulewa, lakini ni adhabu ya Allah iliyo kali.

وَمِنَ النَّاسِ مَنْ يُّجَادِلُ فِي اللّٰهِ بِغَيْرِ عِلْمٍ وَّيَتَّبِعُ كُلَّ شَيْطٰنٍ مَّرِيْدٍ ۙ ④

4. Na katika watu yuko anayebishana juu ya Allah pasipo elimu, na anamfuata kila shetani asi.

كُتِبَ عَلَيْهِ اَنَّهٗ مَنْ تَوَلَّاهُ فَاَنَّهٗ يُضِلُّهٗ وَيَهْدِيْهِ اِلٰى عَذَابِ السَّعِيْرِ ⑤

5. Ameandikiwa ya kwamba atakayemfanya (shetani) kuwa rafiki, kwa yakini yeye atampoteza na kumwongoza kwenye adhabu ya Moto uwakao.

Sura hii imeitwa Haji kwa sababu tangazo la kuhiji ambalo mwanzoni lilitolewa na Nabii Ibrahimu limetangzwa tena kwa dunia nzima na Mtume *s.a.w.* kwa kauli ya Allah iliyomo katika sura hii.

Wafasiri wote wanakubali ya kuwa sehemu kubwa ya sura hii ilishuka Makka ingawa kuna fikira ya kuwa baadhi ya Aya zimeshuka Madina. Ibni Abbas anaona ya kuwa Aya 19-22 zilishuka Madina (Muhit).

Aya 2. *Zalzala*. Neno hili limefasiriwa "mshindo"; maana zake nyingine ni mtetemeko mkubwa, shida na taabu (Taj na Lane).

Aya 4. *Anamfuata kila Shetani asi.* Hapa Shetani mradi wake anaweza kuwa Abu Jahal au Nadhr bin Harth, lakini pia anaweza kuwa mtu ye yote mwenye sifa zilizotajwa hapo.

يٰٓاَيُّهَا النَّاسُ اِنْ كُنْتُمْ فِيْ رَيْبٍ مِّنَ
الْبَعْثِ فَاِنَّا خَلَقْنٰكُمْ مِّنْ تُرَابٍ ثُمَّ
مِنْ نُّطْفَةٍ ثُمَّ مِنْ عَلَقَةٍ ثُمَّ مِنْ مُّضْغَةٍ
مُّخَلَّقَةٍ وَّ غَيْرِ مُخَلَّقَةٍ لِّنُبَيِّنَ لَكُمْ ؕ
وَنُقِرُّ فِي الْاَرْحَامِ مَا نَشَآءُ اِلٰٓى اَجَلٍ
مُّسَمًّى ثُمَّ نُخْرِجُكُمْ طِفْلًا ثُمَّ
لِتَبْلُغُوْٓا اَشُدَّكُمْ ۚ وَمِنْكُمْ مَّنْ يُّتَوَفّٰى
وَمِنْكُمْ مَّنْ يُّرَدُّ اِلٰٓى اَرْذَلِ الْعُمُرِ لِكَيْلَا
يَعْلَمَ مِنْۢ بَعْدِ عِلْمٍ شَيْـًٔا ؕ وَتَرَى الْاَرْضَ
هَامِدَةً فَاِذَآ اَنْزَلْنَا عَلَيْهَا الْمَآءَ اهْتَزَّتْ
وَرَبَتْ وَاَنْۢبَتَتْ مِنْ كُلِّ زَوْجٍۭ بَهِيْجٍ ۝٦

6. Enyi watu! kama mmo katika shaka juu ya ufufuo, basi kwa hakika Tuliwaumbeni kwa udongo, kisha kwa mbegu ya uhai, kisha kwa pande la damu, kisha kwa kipande cha nyama kilichoumbika na kisichoumbika, ili Tuwabainishieni; nasi Tunakikalisha matumboni Tunachokitaka mpaka muda uliowekwa, kisha Tunawatoeni katika hali ya utoto ili baadaye muweze kufikia umri kamili wa utu uzima. Na wapo miongoni mwenu wale ambao hufariki na wapo wengine miongoni mwenu ambao wanarudishwa kwenye umri wa ukongwe hata wanakuwa hawajui kitu baada ya kwishakuwa na elimu. Na unaiona ardhi imechakaa lakini Tunapoyateremsha maji juu yake, inastawi na kurutubika, na huotesha kila namna ya mimea mizuri.

ذٰلِكَ بِاَنَّ اللّٰهَ هُوَ الْحَقُّ وَاَنَّهٗ يُحْيِ الْمَوْتٰى
وَاَنَّهٗ عَلٰى كُلِّ شَيْءٍ قَدِيْرٌ ۝٧

7. Hayo ni kwa sababu Allah ndiye Haki, na ya kwamba Yeye Huwahuisha wafu, na ya kwamba Yeye ni Mwenye uwezo juu ya kila kitu.

وَّاَنَّ السَّاعَةَ اٰتِيَةٌ لَّا رَيْبَ فِيْهَا ۙ وَاَنَّ اللّٰهَ
يَبْعَثُ مَنْ فِي الْقُبُوْرِ ۝٨

8. Na kwa yakini saa ile inafika, haina shaka ndani yake; na kwa hakika Allah Atawafufua waliomo makaburini.

وَمِنَ النَّاسِ مَنْ يُّجَادِلُ فِي اللّٰهِ بِغَيْرِ
عِلْمٍ وَّلَا هُدًى وَّلَا كِتٰبٍ مُّنِيْرٍ ۝٩

9. Na katika watu yuko anayejadiliana juu ya Allah bila elimu, wala mwongozo, wala Kitabu chenye nuru;

Aya 6. Hapa zimeelezwa hali mbalimbali anazopita mwanadamu katika kuumbwa kwake ili kumjulisha jinsi ilivyo dhaifu asili yake, na ya kwamba Mungu aliyempitisha katika hali hizo mbalimbali hata akafika kuwa mtu anaweza pia kumfufua baada ya kufa kwake na jambo hilo si kazi ngumu.

Neno *wanarudishwa* limetumika kuonyesha kwamba kama vile mwanzoni mtoto anavyokuwa dhaifu na asiye na uwezo wa kujiangalia mwenyewe, vivyo hivyo mtu aliye kwenye umri wa ukongwe uliopindukia naye anarudi kwenye hali ya namna hiyo hiyo. Kufanana huku kunaumngwa mkono na ile aya isemayo *wa man nu'amirhu nunakkis-hu fil khaliq* (36:69).

ثَانِيَ عِطْفِهٖ لِيُضِلَّ عَنْ سَبِيْلِ اللّٰهِ ؕ لَهٗ فِي الدُّنْيَا خِزْيٌ وَّنُذِيْقُهٗ يَوْمَ الْقِيٰمَةِ عَذَابَ الْحَرِيْقِ ۝١٠

10. Ageuzaye shingo lake ili kupoteza (watu) katika njia ya Allah. Atapata fedheha duniani na Tutamwonjesha siku ya Kiyama adhabu ya kuungua.

ذٰلِكَ بِمَا قَدَّمَتْ يَدٰكَ وَاَنَّ اللّٰهَ لَيْسَ بِظَلَّامٍ لِّلْعَبِيْدِ ۝١١ ع

11. Hii ni kwa sababu ya yale iliyoyatanguliza mikono yako miwili, na bila shaka Allah si dhalimu kamwe kwa watumishi.

FUNGU 2

وَمِنَ النَّاسِ مَنْ يَّعْبُدُ اللّٰهَ عَلٰى حَرْفٍ ۚ فَاِنْ اَصَابَهٗ خَيْرُ ِۨاطْمَاَنَّ بِهٖ ۚ وَاِنْ اَصَابَتْهُ فِتْنَةُ ِۨانْقَلَبَ عَلٰى وَجْهِهٖ ۚ خَسِرَ الدُّنْيَا وَالْاٰخِرَةَ ؕ ذٰلِكَ هُوَ الْخُسْرَانُ الْمُبِيْنُ ۝١٢

12. Na katika watu yuko anayemwabudu Allah akiwa katika ukingo wa imani; hivyo basi iwapo heri itamfikia hutulia kwayo, na kama atakumbwa na majaribio humgeuzia kisogo Allah. Anapata hasara humu humu duniani na vile vile huko Akhera. Hiyo ndiyo hasara dhahiri.

يَدْعُوْا مِنْ دُوْنِ اللّٰهِ مَا لَا يَضُرُّهٗ وَمَا لَا يَنْفَعُهٗ ؕ ذٰلِكَ هُوَ الضَّلٰلُ الْبَعِيْدُ ۝١٣

13. Humwita badala ya Allah asiyemdhuru wala asiyemfaa. Huo ndiyo upotevu wa mbali.

يَدْعُوْا لَمَنْ ضَرُّهٗۤ اَقْرَبُ مِنْ نَّفْعِهٖ ؕ لَبِئْسَ الْمَوْلٰى وَلَبِئْسَ الْعَشِيْرُ ۝١٤

14. Humwita yule ambaye bila shaka dhara yake i karibu zaidi kuliko nufaa yake. Kwa yakini (huyo) ni mlinzi mbaya na rafiki mbaya.

اِنَّ اللّٰهَ يُدْخِلُ الَّذِيْنَ اٰمَنُوْا وَعَمِلُوا الصّٰلِحٰتِ جَنّٰتٍ تَجْرِيْ مِنْ تَحْتِهَا الْاَنْهٰرُ ؕ اِنَّ اللّٰهَ يَفْعَلُ مَا يُرِيْدُ ۝١٥

15. Bila shaka Allah Atawaingiza wale walioamini na kufanya vitendo vizuri katika Bustani zipitazo mito ndani yao. Hakika Allah Hufanya Atakavyo.

مَنْ كَانَ يَظُنُّ اَنْ لَّنْ يَّنْصُرَهُ اللّٰهُ فِي الدُّنْيَا وَالْاٰخِرَةِ فَلْيَمْدُدْ بِسَبَبٍ اِلَى السَّمَآءِ ثُمَّ لْيَقْطَعْ فَلْيَنْظُرْ هَلْ يُذْهِبَنَّ كَيْدُهٗ مَا يَغِيْظُ ۝١٦

16. Anayedhani ya kwamba Allah Hatamsaidia (Mtume) katika dunia na Akhera, basi na atengeneze njia mbinguni kisha aukate (msaada huo) halafu aone kwamba je mpango wake huo unaweza kuliondoa jambo hilo linalomuudhi?

وَكَذٰلِكَ اَنْزَلْنٰهُ اٰيٰتٍۢ بَيِّنٰتٍ ۙ وَّاَنَّ اللّٰهَ
يَهْدِىْ مَنْ يُّرِيْدُ ﴿١٧﴾

17. Na vivi hivi Tuliiteremsha kuwa Ishara zilizo wazi; na bila shaka Allah Humwongoza Amtakaye.

اِنَّ الَّذِيْنَ اٰمَنُوْا وَالَّذِيْنَ هَادُوْا وَالصّٰبِـُٔوْنَ
وَالنَّصٰرٰى وَالْمَجُوْسَ وَالَّذِيْنَ اَشْرَكُوْٓا ۖ
اِنَّ اللّٰهَ يَفْصِلُ بَيْنَهُمْ يَوْمَ الْقِيٰمَةِ ۭ
اِنَّ اللّٰهَ عَلٰى كُلِّ شَيْءٍ شَهِيْدٌ ﴿١٨﴾

18. Hakika wale walioamini na ambao ni Mayahudi na Wasabii, na Wakristo na Majusi, na wale washirikishao, kwa yakini Allah Atahukumu baina yao siku ya Kiyama; hakika Allah ni Shahidi juu ya kila kitu.

اَلَمْ تَرَ اَنَّ اللّٰهَ يَسْجُدُ لَهٗ مَنْ فِي السَّمٰوٰتِ
وَمَنْ فِي الْاَرْضِ وَالشَّمْسُ وَالْقَمَرُ
وَالنُّجُوْمُ وَالْجِبَالُ وَالشَّجَرُ
وَالدَّوَاۗبُّ وَكَثِيْرٌ مِّنَ النَّاسِ ۭ وَكَثِيْرٌ
حَقَّ عَلَيْهِ الْعَذَابُ ۭ وَمَنْ يُّهِنِ اللّٰهُ فَمَا لَهٗ
مِنْ مُّكْرِمٍ ۭ اِنَّ اللّٰهَ يَفْعَلُ مَا يَشَاۗءُ ﴿١٩﴾ ۧ

19. Je, huoni ya kwamba Allah kinamsujudia kilichomo mbinguni na kilichomo ardhini, na jua na mwezi na nyota na milima, na miti na wanyama, na wengi miongoni mwa watu? Na wengi imewalazimu adhabu. Na ambaye Allah Amemfedhehesha, basi hakuna ampaye heshima. Kwa yakini Allah Hufanya Apendavyo.

هٰذٰنِ خَصْمٰنِ اخْتَصَمُوْا فِيْ رَبِّهِمْ ۡ
فَالَّذِيْنَ كَفَرُوْا قُطِّعَتْ لَهُمْ ثِيَابٌ مِّنْ
نَّارٍ ۭ يُصَبُّ مِنْ فَوْقِ رُءُوْسِهِمُ
الْحَمِيْمُ ﴿٢٠﴾ ۚ

20. Hao wahasimu wawili waliohasimiana juu ya Mola wao; lakini wale waliokufuru watashonewa nguo za Moto; yatamiminwa juu ya vichwa vyao maji yachemkayo.

يُصْهَرُ بِهٖ مَا فِيْ بُطُوْنِهِمْ وَالْجُلُوْدُ ﴿٢١﴾ ۭ

21. Kwayo vitayeyushwa vilivyomo matumboni mwao na ngozi (pia).

وَلَهُمْ مَّقَامِعُ مِنْ حَدِيْدٍ ﴿٢٢﴾

22. Na kwa ajili yao (yatakuwapo) marungu ya chuma.

كُلَّمَآ اَرَادُوْٓا اَنْ يَّخْرُجُوْا مِنْهَا مِنْ
غَمٍّ اُعِيْدُوْا فِيْهَا ۠ وَذُوْقُوْا عَذَابَ
الْحَرِيْقِ ﴿٢٣﴾ ع

23. Kila mara watakapotaka kutoka humo kutokana na simanzi kuu, watarudishwa humo humo na (kuambiwa): Ionjeni adhabu ya kuungua.

Aya 18. Aya hii inaonyesha ya kwamba kuhitilafiana dini hakuleti adhabu kwa wasioamini katika dunia hii. Kinachowaletea adhabu ni uadui wa hao wanaojaribu kuzuia kuineza haki.

Aya 19. Aya hii ina bishara iliyo wazi ya kuwa maadui watadhalilishwa mbele ya Mtume *s.a.w.*

FUNGU 3

24. Hakika Allah Atawaingiza wale walioamini na kufanya vitendo vizuri (katika) Bustani zipitazo mito ndani yake, humo watavishwa bangili za dhahabu, na lulu, na mavazi yao humo yatakuwa hariri,

اِنَّ اللّٰهَ يُدْخِلُ الَّذِيْنَ اٰمَنُوْا وَعَمِلُوا الصّٰلِحٰتِ جَنّٰتٍ تَجْرِيْ مِنْ تَحْتِهَا الْاَنْهٰرُ يُحَلَّوْنَ فِيْهَا مِنْ اَسَاوِرَ مِنْ ذَهَبٍ وَّلُؤْلُؤًا ؕ وَلِبَاسُهُمْ فِيْهَا حَرِيْرٌ ﴿٢٤﴾

25. Na wataongozwa kwenye maneno mazuri tu, na wataongozwa kwenye njia ya Allah Ahimidiwaye.

وَهُدُوْٓا اِلَى الطَّيِّبِ مِنَ الْقَوْلِ ۚ وَهُدُوْٓا اِلٰى صِرَاطِ الْحَمِيْدِ ﴿٢٥﴾

26. Hakika wale waliokataa na kuwazuilia (wengine) njia ya Allah na Msikiti uliotukuzwa ambao Tumeufanya kwa ajili ya watu wote sawasawa, kwa wakaao humo na wageni; na atakayetaka kufanya upotevu humo kwa dhuluma, Tutamwonjesha katika adhabu iumizayo.

اِنَّ الَّذِيْنَ كَفَرُوْا وَيَصُدُّوْنَ عَنْ سَبِيْلِ اللّٰهِ وَالْمَسْجِدِ الْحَرَامِ الَّذِيْ جَعَلْنٰهُ لِلنَّاسِ سَوَآءَ ۨ الْعَاكِفُ فِيْهِ وَالْبَادِ ؕ وَمَنْ يُّرِدْ فِيْهِ بِاِلْحَادٍ بِظُلْمٍ نُّذِقْهُ مِنْ عَذَابٍ اَلِيْمٍ ﴿٢٦﴾ ع

FUNGU 4

27. Na Tulipomtengenezea Ibrahimu mahali pa nyumba takatifu (Kaaba, huku tukisema hivi) ya kwamba usinishirikishe na cho chote, na uisafishe Nyumba Yangu kwa ajili ya wazungukao na wasimamao na wainamao, wasujuduo.

وَاِذْ بَوَّاْنَا لِاِبْرٰهِيْمَ مَكَانَ الْبَيْتِ اَنْ لَّا تُشْرِكْ بِيْ شَيْـًٔا وَّطَهِّرْ بَيْتِيَ لِلطَّآئِفِيْنَ وَالْقَآئِمِيْنَ وَالرُّكَّعِ السُّجُوْدِ ﴿٢٧﴾

28. Na uwatangazie watu habari za Haji, watakufikia kwa miguu na juu ya kila mnyama mkondefu, wakija toka kila njia ya mbali;

وَاَذِّنْ فِي النَّاسِ بِالْحَجِّ يَاْتُوْكَ رِجَالًا وَّعَلٰى كُلِّ ضَامِرٍ يَّاْتِيْنَ مِنْ كُلِّ فَجٍّ عَمِيْقٍ ﴿٢٨﴾ لِّ

Aya 24. Hapa imeelezwa bishara ya kuwa Waislamu watashinda falme kubwa kubwa na hazina za falme hizo zitaingia katika mikono ya Waarabu. Kwa mfano uliposhindwa ufalme wa Ajemi katika siku za Seyidna Umar na hazina za Mfalme Kisra zikaletwa, Seyidna Umar alichukua bangili za dhahabu za mfalme Kisra na akamvisha Suraka kwa sababu Mtume *s.a.w*. alimwambia Suraka, "Utaonaje utakapovaa bangili za Kisra?" (Baihaki na Khasais-ul-Kubra).

Aya 28. *Na utangaze katika watu habari za Haji.* Hii ni bishara tukufu iliyotolewa na

لِّيَشْهَدُوْا مَنَافِعَ لَهُمْ وَيَذْكُرُوا اسْمَ
اللّٰهِ فِيْٓ اَيَّامٍ مَّعْلُوْمٰتٍ عَلٰى مَا رَزَقَهُمْ
مِّنْۢ بَهِيْمَةِ الْاَنْعَامِ ۚ فَكُلُوْا مِنْهَا
وَاَطْعِمُوا الْبَآئِسَ الْفَقِيْرَ ﴿٢٩﴾

29. Ili washuhudie manufaa yao na kulitaja jina la Allah, katika siku maalumu, juu ya yale Aliyowaruzuku katika wanyama wenye miguu minne. Na kuleni katika hao na mlisheni mwenye shida, fakiri.

ثُمَّ لْيَقْضُوْا تَفَثَهُمْ وَلْيُوْفُوْا نُذُوْرَهُمْ
وَلْيَطَّوَّفُوْا بِالْبَيْتِ الْعَتِيْقِ ﴿٣٠﴾

30. Kisha wajisafishe uchafu (wa maovu) yao, na watimize nadhiri zao, na waizunguke Nyumba ya Kale.

ذٰلِكَ ۗ وَمَنْ يُّعَظِّمْ حُرُمٰتِ اللّٰهِ فَهُوَ
خَيْرٌ لَّهٗ عِنْدَ رَبِّهٖ ۗ وَاُحِلَّتْ لَكُمُ
الْاَنْعَامُ اِلَّا مَا يُتْلٰى عَلَيْكُمْ فَاجْتَنِبُوا
الرِّجْسَ مِنَ الْاَوْثَانِ وَاجْتَنِبُوْا
قَوْلَ الزُّوْرِ ﴿٣١﴾

31. Ndivyo hivyo; na anayevitukuza vitu vitakatifu vya Allah, basi hiyo ni heri kwake mbele ya Mola wake. Na mmehalalishiwa wanyama isipokuwa wale mnaosomewa; basi jiepusheni na uchafu wa masanamu na jiepusheni na usemi wa uwongo.

حُنَفَآءَ لِلّٰهِ غَيْرَ مُشْرِكِيْنَ بِهٖ ۗ وَمَنْ
يُّشْرِكْ بِاللّٰهِ فَكَاَنَّمَا خَرَّ مِنَ السَّمَآءِ
فَتَخْطَفُهُ الطَّيْرُ اَوْ تَهْوِيْ بِهِ الرِّيْحُ
فِيْ مَكَانٍ سَحِيْقٍ ﴿٣٢﴾

32. Mhalisike kwa Allah, bila kumshirikisha; na anayemshirikisha Allah basi yu kana kwamba ameporomoka kutoka mbinguni, kisha ndege wamemnyakua au upepo umemtupa mahali pa mbali.

ذٰلِكَ ۗ وَمَنْ يُّعَظِّمْ شَعَآئِرَ اللّٰهِ فَاِنَّهَا
مِنْ تَقْوَى الْقُلُوْبِ ﴿٣٣﴾

33. Ndivyo hivyo; na anayezieheshimu alama za Allah, basi hilo ni katika utawa wa moyo.

لَكُمْ فِيْهَا مَنَافِعُ اِلٰٓى اَجَلٍ مُّسَمًّى
ثُمَّ مَحِلُّهَآ اِلَى الْبَيْتِ الْعَتِيْقِ ﴿٣٤﴾ ع ١١

34. Humo (katika wanyama wa dhabihu) mna manufaa kwa ajili yenu hadi muda maalumu; kisha muwafikishe hadi kwenye Nyumba ya Kale.

Qur'an wakati Mtume *s.a.w.* anafukuzwa Makka na amezuiliwa hata kuifikia Kaaba. Hapa akaambiwa na Allah ya kuwa Uislamu utaenea katika mataifa yote na watu watakuja hata kutoka mbali sana kwa ajili ya kufanya Haji. Ishara hii inatosha kuhakikisha ukweli wa dini ya Kiislamu na kuwa imetoka kwa Allah.

Aya 30. *Nyumba ya Kale* ni Kaaba. Ni nyumba ya zamani sana hata ikawa inajulikana katika bara Arabu yote kwa jina hilo, "Nyumba ya Kale."

FUNGU 5

35. Na kila umati Tumewafanyia mahali pa kutolea sadaka kwa kulitaja jina la Allah juu ya vile Alivyowaruzuku katika wanyama wenye miguu minne; basi Mungu wenu ni Mungu Mmoja, kwa hiyo mjitupe Kwake; na uwaambie habari njema wanyenyekeao,

وَلِكُلِّ اُمَّةٍ جَعَلْنَا مَنْسَكًا لِّيَذْكُرُوا
اسْمَ اللّٰهِ عَلٰى مَا رَزَقَهُمْ مِّنْۢ بَهِيْمَةِ
الْاَنْعَامِ ؕ فَاِلٰهُكُمْ اِلٰهٌ وَّاحِدٌ فَلَهٗۤ
اَسْلِمُوْا ؕ وَبَشِّرِ الْمُخْبِتِيْنَ ۙ﴿۳۵﴾

36. Ambao, Anapotajwa Allah, mioyo yao hutetemeka, na wanavumilia juu ya yale yaliyowasibu na wanasimamisha Sala na katika vile Tulivyowapa wanatoa.

الَّذِيْنَ اِذَا ذُكِرَ اللّٰهُ وَجِلَتْ قُلُوْبُهُمْ
وَالصّٰبِرِيْنَ عَلٰى مَاۤ اَصَابَهُمْ وَالْمُقِيْمِى
الصَّلٰوةِ ۙ وَمِمَّا رَزَقْنٰهُمْ يُنْفِقُوْنَ ﴿۳۶﴾

37. Na ngamia wa sadaka Tumewafanyieni kuwa katika alama za Allah: kwao mnayo heri. Basi litajeni jina la Allah juu yao wasimamapo safu-safu; na waangukapo kibavu; basi kuleni katika hao na mlisheni (fukara) ajizuiaye kuomba na aombaye. Hivyo ndivyo Tumewatiisha kwa ajili yenu ili mpate kushukuru.

وَالْبُدْنَ جَعَلْنٰهَا لَكُمْ مِّنْ شَعَآئِرِ اللّٰهِ
لَكُمْ فِيْهَا خَيْرٌ ۖ فَاذْكُرُوا اسْمَ اللّٰهِ
عَلَيْهَا صَوَآفَّ ۚ فَاِذَا وَجَبَتْ جُنُوْبُهَا
فَكُلُوْا مِنْهَا وَاَطْعِمُوا الْقَانِعَ وَالْمُعْتَرَّ ؕ
كَذٰلِكَ سَخَّرْنٰهَا لَكُمْ لَعَلَّكُمْ
تَشْكُرُوْنَ ﴿۳۷﴾

38. Nyama zao hazimfikii Allah wala damu zao, lakini unamfikia utawa wenu. Hivyo ndivyo

لَنْ يَّنَالَ اللّٰهَ لُحُوْمُهَا وَلَا دِمَآؤُهَا
وَلٰكِنْ يَّنَالُهُ التَّقْوٰى مِنْكُمْ ؕ كَذٰلِكَ

Aya 37. Aya hii na iliyotangulia zikisomwa pamoja zinaonyesha ya kuwa anapochinjwa mnyama litajwe jina la Allah na nyoyo zitetemeke kwa jina Lake, na ikumbukwe ya kuwa uwezo alio nao Allah juu ya mwanadamu ni mkubwa kuliko uwezo alio nao mtu juu ya mnyama anayemchinja, lakini hata hivyo mnyama yuko tayari kufa kwa ajili yake, basi pia mwanadamu kadhalika awe tayari na awe radhi kutoka roho yake kwa ajili ya Allah.

Mlisheni (fukara) aliyekinai na aombaye. Vile Mwislamu anavyotakiwa awe tayari kutoa maisha yake katika dini, pia anatakiwa alishe maskini na kuwasaidia watu katika mambo ya nje. Hapa imeelezwa waziwazi ya kuwa nyama za dhabihu zisifukiwe chini na kutupwa bure bali zitumiwe kwa namna ya kuwafaa watu.

Aya 38. Aya hii inaweka bayana kwamba si habari za nje za sadaka zinazokubaliwa , bali nia safi iliyoko ndani. Tena dhabihu za Kiislamu si fidia inayotolewa kwa ajili ya dhambi za mtu, bali ni tendo linalofanywa na mtu mcha-Mungu ili kutafuta radhi ya Allah.

سَخَّرَهَا لَكُمْ لِتُكَبِّرُوا اللّٰهَ عَلٰى مَا هَدٰىكُمْ ؕ وَ بَشِّرِ الْمُحْسِنِيْنَ ﴿۳۸﴾

Amewatiisha kwenu, ili mumtukuze Allah kwa sababu Amewaongozeni; na uwape habari njema wafanyao hisani.

اِنَّ اللّٰهَ يُدٰفِعُ عَنِ الَّذِيْنَ اٰمَنُوْا ؕ اِنَّ اللّٰهَ لَا يُحِبُّ كُلَّ خَوَّانٍ كَفُوْرٍ ﴿۳۹﴾ ع ۱۳

39. Hakika Allah Huwakingia wale walioamini. Bila shaka Allah Hampendi kila haini mkubwa asiyeshukuru.

FUNGU 6

اُذِنَ لِلَّذِيْنَ يُقٰتَلُوْنَ بِاَنَّهُمْ ظُلِمُوْا ؕ وَ اِنَّ اللّٰهَ عَلٰى نَصْرِهِمْ لَقَدِيْرُ ۙ﴿۴۰﴾

40. Imeruhusiwa (kupigana) kwa wale wanaopigwa, kwa sababu wamedhulumiwa; na kwa yakini Allah Anao uwezo wa kuwasaidia;

Aya 40. Kwa mujibu wa Hadithi zilizo sahihi, hii ndiyo amri ya kwanza kuwaruhusu Waislamu kupigana (Zurkani). Maneno ya Aya hii yanaonyesha waziwazi ya kuwa Waislamu ndio waliopigwa vita kwanza, na tena walikuwa wametaabishwa sana na maadui zao. Tena inaonyesha ya kuwa ruhusa ilipotolewa Waislamu walikuwa dhaifu sana, ndiyo maana Allah anawaambia maneno ya kuwafariji kuwa atawasaidia.

Lakini, jambo linalosikitisha ni kuona ya kuwa fundisho hili la dini ya Kiislamu limekosewa kabisa kufahamiwa hata na baadhii ya Waislamu. Wao wanaeleza juu ya habari za Jihadi mambo ambayo si mafundisho ya Kiislamu hata kidogo, na kwa kufanya hivi wamempa padre silaha ya kuupiga Uislamu. Tunatumai Waislamu hao watafumbua macho yao sasa.

Ukristo ndiwo unaoweza kulaumiwa kwa dhuluma za karaha za namna mbaya kabisa. Yesu aliwaambia, "Msidhani ya kuwa nalikuja kuleta amani duniani; la! sikuja kuleta amani, bali upanga" (Mat 10:34). Maneno haya yanaonyesha kwamba Yesu hakuleta amani bali machafuko. Lakini Wakatoliki katika Injili yao wameshindwa kufanikiwa kujaribu kufasiri maneno haya kuwa mradi wa maneno haya ni wanafunzi wa Yesu kutaabishwa na watu kwa sababu ya kumfuata. Maneno ya Yesu, "Nimeleta upanga" hayakubali tafsiri hiyo. Kadhalika alisema, "Mtu asiye na upanga, auze nguo yake anunue." (Luka 22:36). Maneno haya yanaonyesha waziwazi kuwa anawahimiza wajiandae kwa ajili ya mapigano, siyo wao kuonewa bure kama wateteavyo Wakatoliki.

Ukitazama nyuma katika historia jinsi ma-Papa wa Rumi na maaskofu na wakubwa wa makanisa walivyotumia upanga na moto kwa kuua watu waliohitilafiana nao itikadi, kwa kuwachinja, kwa kuwachoma, kwa kuwatesa mateso ya kila namna, kwa kuwatosa majini, kwa mamia na kwa maelfu, ni mambo ambayo wenye roho ndogo husoma huku miili ikiwatetemeka, mioyo ikiwajaa hofu na huzuni kuwaelemea. Haya yote yanaonekana katika historia walizoandika wenyewe. Watu waliouawa hivi na Wakristo kwa sababu ya dini ni zaidi kuliko 50,000,000. Wajuao Kingereza watafute vitabu hivi na wasome: (1) Historians History of the World jalada la viii, uk. 352. (2) Encyclopaedia of Religions and Ethics, habari za Inquisition. (3) Buck's Theological Dictionary art. Persecutions. (4) Oswald's Kingdom, etc., pp. 107-133. (5) Dowling's History of Romanism. (6) Fox Book of Martyrs. (7) Charlote Elizabeth's Martyrology. (8) The War of the Huguenots (9) The Great Red Dragon. (10) Histories of the Reformation, na vinginevyo, nao wataona ya kuwa hawa walio vinywa wazi kuusingizia Uislamu karaha, historia yao ni nyeusi kabisa haitazamiki.

Lakini Waislamu walifanya nini? Hawakumwangamiza mtu ye yote kwa sababu ya kuhitilafiana naye dini. Waliongamizwa na Waislamu hakika yake ni kwamba walijiangamiza wenyewe. Kwani walipoona Waislamu ni dhaifu, wakaanza kuwaua bure, na wakawanyang'anya mali zao, na kuwafukuza majumbani mwao. Wasikomee hapo, bali Waislamu walipokimbilia Madina, hao maaduia zao wakawafuata kwa majeshi makubwa kuliko wao, na Mayahudi pia wakawa upande wa maadui wa Waislamu. Hapo Allah aliwapa Waislamu amri kupigana na kujitetea kama inavyoonekana katika Aya hii tunayoieleza.

Allah aliwasaidia sana Waislamu, na maadui wao wakashindwa, na wakawa wamejidhulumu wenyewe roho zao kwa kujitia katika janga wasilolijua mwisho wake. Sasa je, ni lawama kwa Waislamu hapa? Tazama jinsi Allah anavyowahimiza Waislamu wajitetee kwa kushika silaha ingawa wenyewe waliona dhiki kupigana. Anasema, "Mmelazishwa kupigana vita ingawa mwaichukia, na huenda mchukie kitu nacho ni heri kwenu, na huenda mpende kitu nacho ni shari kwenu; Allah Anajua lakini ninyi hamjui" (Sura 2:217). Tena Anasema, "Na mna nini hampigani katika njia ya Allah na ya wale walio dhaifu katika wanaume na wanawake na watoto ambao husema: Mola wetu, Ututoe katika mji huu ambao watu wake ni wadhalimu, na Utujaalie mlinzi kutoka Kwako na Utujaalie msaidizi kutoka Kwako" (Sura 4:76).

Aya zilizoko ni nyingi zinazohakikisha wazi kabisa kuwa Waislamu walionewa na kudhulumiwa kwa miaka mingi sana, wakivumilia, wakikimbia, na wakijificha ili wapate salama. Lakini adui alipojihakikisha kuwa hana nia ya kuwaacha huru wafuate dini yao, na amekazana tu kuwafuata, basi Allah Aliwaamrisha Waislamu dhaifu wajitetee. Basi hapo kila namna ya ajali iliyowakumba makafiri walikuwa wameistahili, maana wao ndio walikuwa wadhalimu.

Hiyo ndiyo hakika ya vita vya Waislamu, ambavyo hata Waandishi wa Ulaya waliopeleleza kwa nia safi wanakubali kuwa Waislamu waliamrishwa kupigana tu adui alipokuwa ni wa kwanza kushika silaha kuwashambulia. Wameandika, "Hata hivyo, Vita Takatifu hailazimishwi isipokuwa, na ni kwa hilo tu, endapo maadui wa Uislamu wameleta vita. Ni tafsiri tu za kigeugeu zinazotolewa na wanazuoni wa dini ambazo zinageuza habari hii iende kinyume" (Historians History of the World, Vol. viii, pp. 270).

Tena wameandika, "Kosa jingine lililo sawa na hilo ni kudhani ya kwamba Uislamu umeenezwa kwa nguvu. Utawala wa nchi ndiyo umeenea kwa njia hiyo, si dini. Makhalifa, mbali na kutafuta kuwasilimisha watu kwa ajili ya faida ya pesa, hawakupendezwa na kuona watu walioshindwa wakiingia dini" (vol. viii, pp. 270). Hiyo ndiyo hali ya vita zilizoagizwa na Qur'an. Na sasa tuone Waislamu walipigana vita hizo kwa adabu gani, na kisha linganisheni na mapigano ya watu wa kitabu cha Biblia mtakayosoma baadaye kidogo.

Kabla ya Waislamu kupigana na maadui waliowapelekea vita, Mtume *s.a.w.* aliwaamuru wawape masharti matatu ya kutaka amani: (1) "Waiteni waingie Uislamu, na wakikubali, basi wasadikini na mzuie mikono yenu; (2) kisha washawishini wahamie Madina, ambako watapata haki zote za Wahamaji, nanyi mtachukua madaraka yao; lakini wakikataa kuhamia Madina basi watakosa haki na nafuu za kuhamia Madina, ingawa watafahamiwa na kutendewa kama Waislamu; (3) wakikataa kuingia Uislamu, basi watakeni wakae chini ya ulinzi wa Serikali ya Kiislamu na wakubali kulipa kodi. Lakini wakikataa mojawapo katika masharti haya matatu, basi mtegemeeni Allah na anzeni kupigana nao" (Muslim).

Hii ndiyo juhudi iliyofanywa na Waislamu hata katika uwanja wa vita kuepuka mapigano yaliyoletwa na maadui. Lakini kama adui hataki kuacha vita, sasa tufanyeje, tukae kimya tu tuuawe kama kuku na mbuzi au tuwanie roho zetu na kujitetea? Hapa tunatoa vitabu vya Wakristo vijibu swali hilo: "Rudisha upanga wako mahali pake; maana wote waushikao upanga, wataangamia kwa upanga" (Matt. 26:52); "Mtu akiua kwa upanga, atauawa kwa upanga" (Ufunuo 13:10); Atakayemwaya damu ya bin-Adamu, damu yake huyo itamwaywa na bin-Adamu" (Mwanzo 9:6).

Tena Mtume *s.a.w.* aliwaagiza Waislamu wanapokwenda vitani akasema, "Fanyeni vita kwa jina la Mungu na piganeni katika njia ya Allah, wala msidanganye, wala msivunje mapatano, wala msiwakatekate waliouawa, wala msiwaue watoto, au wanawake na watu wanaokaa katika makanisa na mamonaki" (Muslim, Tahaawi, Abu Daud). Na Seyidna Abu Bakar Khalifa wa kwanza wa Mtume *s.a.w.,* alikuwa akiwaagiza majemedari wake hivi, "Mnapokutana na maadui zenu, jitoeni kama wanaume, wala msiwape migongo; na manaposhinda, basi msiwaue watoto, wala wazee wala wanawake. Msikate mitende wala msichome mashamba. Msikate miti ya matunda wala msiwaue wanyama isipokuwa wale mnaochinja kwa ajili ya chakula. Mnapofanya mapatano basi yashikeni na yatimizeni. Mnapoendelea mtawakuta watu wa dini waliotulia katika mamonaki yao, ambao wamejichagulia kumtumikia Mungu namna hiyo. Waacheni, msiwaue wala msiharibu majumba yao" (Mu'atta Imam Malik).

Sasa tugeukie vita zilizoagizwa na Biblia, Kitabu kitakatifu cha Wakristo. Vita za Biblia zilikuwa za uchokozi na uuaji wa bure ulio mbaya kupita kiasi. Anayesoma Biblia juu ya habari za vita za Daudi, na wana wa Israeli wengine kama Yoshua, hangefikiri kuwa hawa mapadre wangesahau uovu ulio nyumbani mwao na kuanza kuilaumu dini ya Kiislamu bure. Kitabu chao kinawaambia waendapo kuupiga mji vita, kwanza wautake ujisalimishe mikononi mwao. Ukijisalimisha na kuwafungulia milango, hapo wawafanye watu wote waliomo humo mjini kuwa watumwa wao (Kumbukumbu 20:11). Lakini kama mji huo ukikataa kuonewa bure na watu wajaribu kujitetea kwa mapigano, basi watu hao wakishindwa, wanaume wote wachinjwe, na wanawake na watoto watiwe utumwani na vitu vingine vitekwe nyara (Kumbukumbu 20:14).

Amri hizo ni kwa miji ya mbali. Lakini kama miji hiyo ni ya karibu ambayo Mungu wao anataka wao waichukue, basi humo wanaambiwa wasiache hai "cho chote kinachovuta pumzi" ndiyo kusema waue watu, wanyama, ndege, wadudu, na kila kitu kinachovuta pumzi (Kumbukumbu 20:16) Ukatili wa namna hii dunia ndio kwanza iusikie ndani ya vitabu vya Kikristo. Na pia waliambiwa wakiwashinda mataifa saba ya Wahitti, Wagirgashi, Waamori, Wakanaani, Waperizi, Wahivi na Wajebusi, wawachinje wote - *wote* kabisa! bila kufanya nao mapatano yo yote (Kumbukumbu 7:2). Na babu ya Yesu Kristo, Daudi, aliua watu 22,000 (ishirini na mbili elf) katika dafaa moja (2 samuel 8:5). Na Yoshua aliuvamia mji wa Ai hali wenyeji hawana habari, wakauchoma moto, na kuwaua wenyeji wote waliokuwamo, wanawake, wazee na watoto pia - ndiko kuua kwao. Watu waliojaribu kukimbia waliandamwa na kukamatwa na kuuawa. watu wote waliouawa siku ile walikuwa 12,000. Mfalme alitungikwa, na alipokufa, badala ya kuzikwa kama mtu, aliwekwa mahali wakamkandamiza na lundo kubwa la mawe. Biblia inasema mji wa Ai ulikufa mpaka leo na lundo hilo la mawe liko mpaka leo (Yoshua 8:21-29).

Malinganisho haya kidogo yatamfahamisha msomaji ya kuwa dini inayostahili kulaumiwa kwa vita za uchokozi na karaha na ukatili ni dini inayofuata Kitabu cha Biblia.

Zaidi ya hayo, Mtume *s.a.w.* alitoa mkataba wa uhuru wa dini kwa Mayahudi, Mazartashti na Wakristo. Hapa chini tunanakili hati ya uhuru wa dini walioandikiwa Wakristo bila wao kuomba, na oneni wenyewe jinsi Mtume Muhammad *s.a.w*. alivyowafadhili Wakristo waliokuwa chini ya mamlaka yake, na anavyowagiza Waislamu wawatendee mpaka siku ya Kiyama. Hati hiyo inasema hivi:

"Hii ni hati ambayo Muhammad Bin Abdallah, Mtume wa Allah. Mwonyaji na Mletaji wa habari njema, ameandikisha, ili pasibakie udhuru wo wote kwa hao watakaokuja baadaye. Nimeandikisha hati hii kwa ajili ya Wakristo wa Mashariki na Magharibi, kwa ajili yao wakaao karibu na hao wakaao nchi za mbali, kwa Wakristo walio hai sasa na hao watakaokuja baadaye, kwa ajili ya Wakristo wanaojulikana kwetu na pia hao tusiowajua. Mwislamu ye yote atakayevunja na kupuuza yaliyoamrishwa ndani yake atafahamiwa ni mvunjaji wa agano la Mungu na atakuwa ni mvunjaji wa ahadi Yake na atajifanya astahili laana ya Mungu, akiwa mfalme au raia.

"Ninaahidi ya kuwa mmonaki ye yote au mpita njia n.k.w. atakayetaka msaada wangu juu ya milima, katika misitu, majangwa au mnamokaliwa na watu, na katika mwahali mwa ibada,

nitawafukuza maadui zake pamoja na rafiki zangu wote na wasaidizi wangu, pamoja na jamaa zangu wote na pamoja na hao wanaodai kunifuata, na kumlinda, kwa sababu wao ni raia zangu nami ninawapa kuwakinga, yaani wako juu ya agano langu. Nami nitawalinda waliopewa agano wasiteswe, wasijeruhiwe na wasisumbuliwe na maadui zao, na kwa hayo watalipa kodi (jizya) ambayo wameahidi kutoa.

"Wakipendelea kulinda mali zao na nafsi zao wenyewe, wataruhusiwa kufanya hivyo na hawatapewa uzito wo wote kwa jambo hilo. Hakuna askofu atakayefukuzwa katika mamlaka yake, wala mmonaki katika monaki yake na wala kasisi katika mahali pake pa ibada, na hakuna mhaji atakayezuiwa katika haji yake. Makanisa yao na mwahali mwingine mwa ibada havitanyang'anywa au kuangamizwa au kuvunjwa. Vifaa vya makanisa yao havitatumiwa kwa kujengea misikiti au majumba ya Waislamu. Mwislamu ye yote atakayefanya hivyo afahamiwe amemwasi Mungu na Mtume Wake. Mamonaki na maaskofu hawatatozwa kodi (jizya) au ukombozi na wakae misituni au mitoni, wawe mashariki au magharibi, kaskazini au kusini. Ninawapa ahadi yangu. Wako juu ya ahadi yangu na agano langu na watakaa kwa salama kabisa wasipate kila namna ya udhia. Wanaokaa milimani na mwahali mwa wakfu mazao ya mashamba yao hayatatozwa kodi, na katika nyakati za upungufu wa chakula hawatalazimishwa kutoa cho chote katika nafaka kuwa mchango. Hawatafanyishwa kazi za vita, wala hawatatozwa jizya. Dirham zisizozidi 12 kwa mwaka watatozwa wafanyi biashara wao na wanaomiliki ardhi na matajiri miongoni mwao. Wasisumbuliwe na kufanyiwa jeuri kwa kulipa kodi. Katika mijadala na mashindano ya dini wazungumzwe kwa adabu na upole. Basi rehema iwafunike po pote walipo na walindwe na kila namna ya taabu na udhia. Aliyevunja agano la Mungu na kufanya ushindani atafahamiwa ni adui wa Mungu na mvunjaji wa agano Lake. Wapewe kila namna ya msaada katika kutengeneza makanisa yao yanapoharibika. Watapewa uhuru wa kutochukua silaha. Watalindwa na Waislamu. Basi hati hii isikose kutiiwa mpaka siku ya Kiyama." (Futuh-ul-Bu dan Balazar).

Kwa neno zima, Uislamu haukupigana vita ili kueneza dini. Dini ya Kiislamu toka mwanzo imehubiriwa kwa njia za amani kabisa, zisizo za karaha, kama wanavyoshuhudia waandishi wafuatao, ambao wenyewe si Waislamu:-

George Sale ameandika juu ya kazi ya Mtume *s.a.w.* ya kuhubiri dini ya wakati wa Mtume *s.a.w.* alipokuwa angali Makka, na amesema, Mtume "anatangaza kazi yake ilikuwa kuhubiri tu na kuonya; ya kwamba hakuwa na mamlaka ya kumlazimisha mtu ye yote kufuata dini yake; na ya kwamba watu wakiamini au wasiamini si shauri lake, bali ni shauri la Mungu tu. Na alikuwa mbali kabisa na kuwaruhusu wafuasi wake nguvu hata akawanasihi kuvumilia kwa subira majeraha haya waliyotiwa kwa ajili ya dini yao; na, yeye mwenyewe alipoteswa, akachagua afadhali kuondoka mahali alipozaliwa na kukaa Madina kuliko kufanya ushindani wa namna yo yote" (Preliminary Discourse of the Translation of the Holy Quran).

Mtume *s.a.w.* aliendesha kazi yake ya kuhubiri kwa amani Madina kama alivyofanya Makka. Mwanachuoni mwingine Mzungu ameandika: "Baada ya Hijra, juhudi za namna ile ile kabisa zilifanywa ili kuuhubiri Uislamu kwa Waarabu wasioamini kama vile kwanza katika siku Muhammad alipokuwa hana nguvu katika mambo ya utawala." (Preaching of Islam by T. W. Arnold).

Makafiri walipoleta vita kuwashambulia Waislamu Madina, Mtume *s.a.w.* alilazimika kutoka na kupambana nao. T. W. Arnold ameandika, "Kwa hiyo Muhammad hawezi kulaumiwa kwa kutoka kwenda kutana nao kwa ajili ya kuulinda mji uliompa makao yeye na wafuasi wake, ili kuuokoa na maafa ya kuhusuriwa, ambayo kwa hali ya Madina ilivyo, mji ungelazimika kuteseka vikali" (Preaching of Islam).

Bwana T. W. Arnold ameendelea kueleza ya kwamba haikupata kutokea Uislamu kusilimisha watu kwa nguvu. Anasema, "Toka mwanzo kabisa Uislamu unayo chapa ya kuonyesha kwamba ni dini ya kuhubiri inayotaraji kuishinda mioyo ya watu, na kuwageuza na kuwanasihi waingie katika udugu wa waaminio; na kama ulivyokuwa mwanzoni, ndivyo ambavyo umeendelea kuwa mpaka siku ya leo" (The Preaching of Islam).

41. Waliotolewa majumbani mwao pasipo haki ila kwa sababu tu wanasema: Mola wetu ni Allah. Na kama Allah Asingaliwazuia watu, baadhi yao kwa wengine, bila shaka yangalivunjwa mahekalu na makanisa, na nyumba za ibada na misikiti ambamo jina la Allah hutajwa kwa wingi. Na bila shaka Allah Humsaidia

الَّذِيْنَ اُخْرِجُوْا مِنْ دِيَارِهِمْ بِغَيْرِ حَقٍّ
اِلَّآ اَنْ يَّقُوْلُوْا رَبُّنَا اللّٰهُ ؕ وَلَوْلَا دَفْعُ اللّٰهِ
النَّاسَ بَعْضَهُمْ بِبَعْضٍ لَّهُدِّمَتْ
صَوَامِعُ وَبِيَعٌ وَّصَلَوٰتٌ وَّ مَسٰجِدُ
يُذْكَرُ فِيْهَا اسْمُ اللّٰهِ كَثِيْرًا ؕ وَلَيَنْصُرَنَّ

Mwandishi mwingine Mzungu, W. Thomson, ameandika, "Mvamio wa kustaajabisha wa majeshi ya Waarabu mashariki na magharibi unaonekana ulizileba akili za waandishi wa historia wa Kikristo. Lakini kusema ya kuwa Uislamu ulienea kwa upanga, kama wasemavyo wengi zaidi kati yao, ndiyo mashtaka makubwa kwa Muhammad na wafuasi wake, ambayo nguvu hii isiyoshindika ya uhodari wa vita tu haitoshi kuyapa haki mashtaka hayo, ambayo kwa hakika yanabatilishwa na ushahidi wa historia ya Waarabu na pia yanabatilishwa na mafundisho ya Qur'an yenyewe" (The Muslim World).

Dr. E. J. Byng ameandika, "Hakuna kitu kingekuwa cha maana zaidi katika jambo hili kuliko hakika inayostaajabisha ya kwamba leo, ambapo Waislamu walio wengi zaidi kabisa wako katika kutawaliwa na serikali za Kikristo, Uislamu uendelee kuwa zaidi sana dini yenye nguvu kabisa ya kuongoa watu. Idadi ya Wachina, watu wa visiwa vya South Sea na watu wengine ambao wahubiri wa Kikristo wanawatia Ukristo ni ndogo kwa kulinganishwa na malaki na malaki hasa katika Afrika, ambao, mwaka hata mwaka wanaingia Uislamu kwa hiari zao. Kuna vyama kadha wa kadha vya Waislamu huko mashariki vya kuhubiri dini. Hakuna serikali inayowasaidia. Lakini mhubiri wa Kikristo anao msaada usio na mpaka wa serikali yake. Juu ya hayo Uislamu unaendelea na mwendo wake uliouanza karne kumi na tatu zilizopita" (The World of the Arabs).

Hiyo ndiyo kweli. Ukiangalia juhudi za Mwendeleo wa Ahmadiyya katika Uislamu, hutakosa kuathiriwa na nguvu hii ya kimwujiza ya Uislamu. Waahmadiyya wamesimika kazi za kuhubiri Uislamu kila mahali duniani. Waamerika maelfu kwa maelfu na kadhalika Wazungu wa Ulaya, wameingia katika Uislamu kwa juhudi zetu, hata baadhi yao wamejitolea katika kazi za kuhubiri Uislamu na kuueneza kati ya jamaa zao. Maelfu na maelfu ya Waafrika katika Gold Coast (Ghana), Nigeria, Sierra Leone, na Afrika Mashariki wameingia Uislamu kwa juhudi hii. Maelfu na maelfu ya watu katika Java, Smatra, Indonesia, Straight Settlements, na kila upande wa dunia, wanaingia Uislamu kwa kazi ile ile iliyoanzwa na Mtume Muhammad *s.a.w.* mika 1,400 iliyopita. Naam, dunia nzima imewekewa siku mbele ya Allah itakapoacha Ukristo, Ubaniani na kila dini zenye giza, nayo itapiga magoti kwa heshima na unyenyekevu mbele ya Qur'an na Mtume Muhammad *s.a.w.* hali wamejaa hamu ya kurejea kwa Mola wao Allah. Na kazi hii inafanyika na itafanyika kama ilivyofanyika hapo kwanza bila shuruti, bila karaha, bila nguvu na bila namna yo yote ya tashtiti; na dunia itakiri utukufu wa kweli hii inayoelezwa ya kuwa, naam Uislamu unayo nguvu ya kuwavuta watu na kuwaongoa, kimya bila matata, leo, kama ulivyokuwa zamani.

Aya 41. *Waliotolewa majumbani mwao pasipo haki,* mradi wake ni Waislamu waliolazimika kukimbilia Abisinia au kuhamia Madina na kuacha majumba yao na mali zao kwa sababu ya fitina ya makafiri.

yule anayemsaidia Yeye; hakika Allah ni Mwenye nguvu, Mshindi;

42. Wale ambao Tukiwaimarisha katika ardhi watasimamisha Sala na watatoa Zaka na wataamrisha yaliyo mema na watakataza yaliyo mabaya; na mwisho wa mambo yote u mikononi mwa Allah.

43. Na kama wakikukadhibisha, basi walikadhibisha kabla yao watu wa Nuhu na Waadi na Wathamudi,

44. Na watu wa Ibrahimu na watu wa Luti,

45. Na watu wa Madiani, na Musa pia alikadhibishwa. Lakini Niliwapa muda makafiri kisha Nikawakamata, basi lo, ilikuwaje adhabu Yangu!

46. Basi ni miji mingapi Tuliiangamiza hali ikidhulumu, nayo ikaangukiwa na mapaa yake; na visima (vingapi) vilivyoachwa na makasri (yaliyokuwa) madhubuti?

47. Je, hawatembei katika ardhi ili wapate mioyo ya kufahamia, au masikio ya kusikilia? Kwa hakika macho hayakupofuka, bali ni mioyo imepofuka ambayo imo vifuani.

48. Na wanakuomba uilete adhabu kwa haraka, lakini Allah Hatavunja ahadi Yake; na bila shaka, kwa Mola wako, iko pia siku inayofanana na miaka elfu mnayoihesabu.

اللّٰهُ مَنۡ يَّنۡصُرُهٗ ؕ اِنَّ اللّٰهَ لَقَوِىٌّ عَزِيۡزٌ ﴿۴۱﴾
اَلَّذِيۡنَ اِنۡ مَّكَّنّٰهُمۡ فِى الۡاَرۡضِ اَقَامُوا الصَّلٰوةَ وَاٰتَوُا الزَّكٰوةَ وَاَمَرُوۡا
بِالۡمَعۡرُوۡفِ وَنَهَوۡا عَنِ الۡمُنۡكَرِ ؕ
وَلِلّٰهِ عَاقِبَةُ الۡاُمُوۡرِ ﴿۴۲﴾
وَاِنۡ يُّكَذِّبُوۡكَ فَقَدۡ كَذَّبَتۡ قَبۡلَهُمۡ
قَوۡمُ نُوۡحٍ وَّعَادٌ وَّثَمُوۡدُ ﴿۴۳﴾
وَقَوۡمُ اِبۡرٰهِيۡمَ وَقَوۡمُ لُوۡطٍ ﴿۴۴﴾
وَّاَصۡحٰبُ مَدۡيَنَ ۚ وَكُذِّبَ مُوۡسٰى
فَاَمۡلَيۡتُ لِلۡكٰفِرِيۡنَ ثُمَّ اَخَذۡتُهُمۡ ۚ
فَكَيۡفَ كَانَ نَكِيۡرِ ﴿۴۵﴾
فَكَاَيِّنۡ مِّنۡ قَرۡيَةٍ اَهۡلَكۡنٰهَا وَهِىَ
ظَالِمَةٌ فَهِىَ خَاوِيَةٌ عَلٰى عُرُوۡشِهَا وَبِئۡرٍ
مُّعَطَّلَةٍ وَّقَصۡرٍ مَّشِيۡدٍ ﴿۴۶﴾
اَفَلَمۡ يَسِيۡرُوۡا فِى الۡاَرۡضِ فَتَكُوۡنَ لَهُمۡ
قُلُوۡبٌ يَّعۡقِلُوۡنَ بِهَاۤ اَوۡ اٰذَانٌ يَّسۡمَعُوۡنَ
بِهَا ۚ فَاِنَّهَا لَا تَعۡمَى الۡاَبۡصَارُ وَلٰكِنۡ
تَعۡمَى الۡقُلُوۡبُ الَّتِىۡ فِى الصُّدُوۡرِ ﴿۴۷﴾
وَيَسۡتَعۡجِلُوۡنَكَ بِالۡعَذَابِ وَلَنۡ يُّخۡلِفَ
اللّٰهُ وَعۡدَهٗ ؕ وَاِنَّ يَوۡمًا عِنۡدَ رَبِّكَ كَاَلۡفِ
سَنَةٍ مِّمَّا تَعُدُّوۡنَ ﴿۴۸﴾

Watu wanaoishitaki dini ya Kiislamu kuwa ina kero kwa dini zingine waangalie Aya hiyo, kisha watazame ni uhuru wa namna gani waliopewa watu wa dini zingine wakati Islam ilipotawala katika bara Arabu. Waislamu wanaambiwa hata wawe tayari kufa katika kulinda majumba ya ibada ya dini zingine. Je, kuna dini yo yote inayotoa mafundisho kama haya?

49. Na miji mingapi Niliyoipa muda na hali ilikuwa ikidhulumu? Kisha Niliwakamata: na Kwangu ndiko marudio.

وَكَاَيِّنْ مِّنْ قَرْيَةٍ اَمْلَيْتُ لَهَا وَهِيَ ظَالِمَةٌ ثُمَّ اَخَذْتُهَا ۚ وَاِلَيَّ الْمَصِيْرُ ﴿٤٨﴾

FUNGU 7

50. Sema: Enyi watu! Bila shaka mimi kwa ajili yenu ni Mwonyaji dhahiri.

قُلْ يٰٓاَيُّهَا النَّاسُ اِنَّمَآ اَنَا لَكُمْ نَذِيْرٌ مُّبِيْنٌ ﴿٤٩﴾

51. Basi wale walioamini na wakafanya vitendo vizuri watapata msamaha na riziki yenye heshima.

فَالَّذِيْنَ اٰمَنُوْا وَعَمِلُوا الصّٰلِحٰتِ لَهُمْ مَّغْفِرَةٌ وَّرِزْقٌ كَرِيْمٌ ﴿٥٠﴾

52. Na wale waliojitahidi kuzidhoofisha Aya Zetu, hao ndio watu wa motoni.

وَالَّذِيْنَ سَعَوْ فِيْٓ اٰيٰتِنَا مُعٰجِزِيْنَ اُولٰٓئِكَ اَصْحٰبُ الْجَحِيْمِ ﴿٥١﴾

53. Na Hatukumtuma kabla yako Mtume wala Nabii ila alipotamani, Shetani alitia (fitina) katika tamanio lake. Lakini Allah Huondoa anayoyatia Shetani, kisha Allah Huziimarisha Ishara Zake; na Allah ni Mjuzi, Mwenye hekima.

وَمَآ اَرْسَلْنَا مِنْ قَبْلِكَ مِنْ رَّسُوْلٍ وَّلَا نَبِيٍّ اِلَّآ اِذَا تَمَنّٰٓى اَلْقَى الشَّيْطٰنُ فِيْٓ اُمْنِيَّتِهٖ ۚ فَيَنْسَخُ اللّٰهُ مَا يُلْقِى الشَّيْطٰنُ ثُمَّ يُحْكِمُ اللّٰهُ اٰيٰتِهٖ ۗ وَاللّٰهُ عَلِيْمٌ حَكِيْمٌ ﴿٥٢﴾

54. (Hufanyika haya) ili Alifanye lile analotia Shetani kuwa jaribio kwa wale wenye maradhi mioyoni mwao na ambao mioyo yao ni migumu; na bila shaka wadhalimu wamo katika upinzani wa mbali,

لِّيَجْعَلَ مَا يُلْقِى الشَّيْطٰنُ فِتْنَةً لِّلَّذِيْنَ فِيْ قُلُوْبِهِمْ مَّرَضٌ وَّالْقَاسِيَةِ قُلُوْبُهُمْ ۗ وَاِنَّ الظّٰلِمِيْنَ لَفِيْ شِقَاقٍ بَعِيْدٍ ﴿٥٣﴾

55. Na ili wajue wale waliopewa elimu ya kwamba hiyo ni haki iliyotoka kwa Mola wako na waiamini, na ili inyenyekee Kwake mioyo yao; na kwa yakini Allah ndiye Awaongozaye wale walioamini kwenye njia iliyonyooka.

وَّلِيَعْلَمَ الَّذِيْنَ اُوْتُوا الْعِلْمَ اَنَّهُ الْحَقُّ مِنْ رَّبِّكَ فَيُؤْمِنُوْا بِهٖ فَتُخْبِتَ لَهٗ قُلُوْبُهُمْ ۗ وَاِنَّ اللّٰهَ لَهَادِ الَّذِيْنَ اٰمَنُوْٓا اِلٰى صِرَاطٍ مُّسْتَقِيْمٍ ﴿٥٤﴾

Aya 53. Sio mradi wa Aya hii kwamba Shetani anaweza kupenyeza maneno yake wakati Mtume wa Allah anasoma ufunuo anaoteremshiwa. Mradi wa maneno haya ni kwamba

وَلَا يَزَالُ الَّذِيْنَ كَفَرُوْا فِيْ مِرْيَةٍ مِّنْهُ حَتّٰى تَاْتِيَهُمُ السَّاعَةُ بَغْتَةً اَوْ يَاْتِيَهُمْ عَذَابُ يَوْمٍ عَقِيْمٍ ﴿٥٥﴾

56. Na wataendelea wale waliokufuru kuwa katika wasiwasi kwa hilo mpaka saa ile itawafikia kwa ghafla, au itawafikia adhabu ya siku yenye mkosi.

اَلْمُلْكُ يَوْمَئِذٍ لِّلّٰهِ ؕ يَحْكُمُ بَيْنَهُمْ ؕ فَالَّذِيْنَ اٰمَنُوْا وَعَمِلُوا الصّٰلِحٰتِ فِيْ جَنّٰتِ النَّعِيْمِ ﴿٥٦﴾

57. Ufalme siku hiyo utakuwa wa Allah; Atahukumu baina yao. Basi wale walioamini na wakafanya vitendo vizuri watakuwa katika Bustani zenye neema.

وَالَّذِيْنَ كَفَرُوْا وَكَذَّبُوْا بِاٰيٰتِنَا فَاُولٰٓئِكَ لَهُمْ عَذَابٌ مُّهِيْنٌ ﴿٥٧﴾ ع ١٤

58. Na wale waliokufuru na kuzikadhibisha Ishara Zetu, basi hao watapata adhabu ifedheheshayo.

FUNGU 8

وَالَّذِيْنَ هَاجَرُوْا فِيْ سَبِيْلِ اللّٰهِ ثُمَّ قُتِلُوْٓا اَوْ مَاتُوْا لَيَرْزُقَنَّهُمُ اللّٰهُ رِزْقًا حَسَنًا ؕ وَاِنَّ اللّٰهَ لَهُوَ خَيْرُ الرّٰزِقِيْنَ ﴿٥٨﴾

59. Na wale waliohama katika njia ya Allah kisha wakauawa au wakafa, bila shaka Allah Atawaruzuku riziki njema; na hakika Allah ni Mbora wa wanaoruzuku.

لَيُدْخِلَنَّهُمْ مُّدْخَلًا يَّرْضَوْنَهٗ ؕ وَاِنَّ اللّٰهَ لَعَلِيْمٌ حَلِيْمٌ ﴿٥٩﴾

60. Kwa yakini Atawaingiza mahali watakapoparidhia; na bila shaka Allah ni Mjuzi, Mpole.

ذٰلِكَ ۚ وَمَنْ عَاقَبَ بِمِثْلِ مَا عُوْقِبَ بِهٖ ثُمَّ بُغِيَ عَلَيْهِ لَيَنْصُرَنَّهُ اللّٰهُ ؕ اِنَّ اللّٰهَ لَعَفُوٌّ غَفُوْرٌ ﴿٦٠﴾

61. Ndivyo hivyo, na ajilipizaye kisasi sawa na dhara aliyotiwa, naye kadhulumiwa, bila shaka Allah Atamsaidia. Hakika Allah ni Msamehevu, Mwenye ghofira.

ذٰلِكَ بِاَنَّ اللّٰهَ يُوْلِجُ الَّيْلَ فِي النَّهَارِ وَيُوْلِجُ النَّهَارَ فِي الَّيْلِ وَاَنَّ اللّٰهَ سَمِيْعٌۢ بَصِيْرٌ ﴿٦١﴾

62. Hayo ni kwa sababu Allah Huingiza usiku katika mchana, na Huingiza mchana katika usiku, na ya kwamba Allah ni Asikiaye, Aonaye.

matamanio ya Mtume huwa kueneza haki kwa watu. Shetani matamanio yake ni kuwa hataki haki ienee, Basi anawachochea watu kuipinga kazi ya Mtume; lakini mwishoni Allah huondoa fujo ya Shetani na kweli ikasimamishwa.

ذٰلِكَ بِاَنَّ اللّٰهَ هُوَ الْحَقُّ وَاَنَّ مَا يَدْعُوْنَ
مِنْ دُوْنِهٖ هُوَ الْبَاطِلُ وَاَنَّ اللّٰهَ هُوَ الْعَلِيُّ
الْكَبِيْرُ ﴿٦٢﴾

63. Hayo ni kwa sababu Allah ndiye Haki, na ya kwamba wanaowaita badala ya Yake huo ndiyo uwongo, na ya kwamba Allah ndiye Aliye juu, Mkubwa.

اَلَمْ تَرَ اَنَّ اللّٰهَ اَنْزَلَ مِنَ السَّمَآءِ مَآءً ۖ
فَتُصْبِحُ الْاَرْضُ مُخْضَرَّةً ۭ اِنَّ اللّٰهَ
لَطِيْفٌ خَبِيْرٌ ﴿٦٣﴾

64. Je, huoni ya kwamba Allah Ameteremsha maji kutoka mawinguni na ardhi ikawa chanikiwiti? Hakika Allah ni Latifu, Mwenye habari.

لَهٗ مَا فِي السَّمٰوٰتِ وَمَا فِي الْاَرْضِ ۭ وَاِنَّ
اللّٰهَ لَهُوَ الْغَنِيُّ الْحَمِيْدُ ﴿٦٤﴾

65. Ni Vyake vilivyomo mbinguni na vilivyomo ardhini. Na hakika Allah ni Mkwasi, Asifiwaye.

FUNGU 9

اَلَمْ تَرَ اَنَّ اللّٰهَ سَخَّرَ لَكُمْ مَّا فِي الْاَرْضِ
وَالْفُلْكَ تَجْرِيْ فِي الْبَحْرِ بِاَمْرِهٖ ۭ
وَيُمْسِكُ السَّمَآءَ اَنْ تَقَعَ عَلَي الْاَرْضِ
اِلَّا بِاِذْنِهٖ ۭ اِنَّ اللّٰهَ بِالنَّاسِ لَرَءُوْفٌ
رَّحِيْمٌ ﴿٦٥﴾

66. Je, hukuona kwamba Allah Amevitiisha kwa ajili yenu vilivyomo ardhini, na merikebu zinazopita baharini kwa amri Yake, na Anazizuia sayari za angani zisiiangukie ardhi ila kwa idhini yake. Kwa yakini Allah ni Raufu na Mrehemevu kwa watu.

وَهُوَ الَّذِيْٓ اَحْيَاكُمْ ۡ ثُمَّ يُمِيْتُكُمْ ثُمَّ
يُحْيِيْكُمْ ۭ اِنَّ الْاِنْسَانَ لَكَفُوْرٌ ﴿٦٦﴾

67. Naye ndiye Aliyewahuisheni kisha Atawafisheni, kisha Atawafufueni. Hakika mwanadamu ni mwenye kukufuru sana.

لِكُلِّ اُمَّةٍ جَعَلْنَا مَنْسَكًا هُمْ نَاسِكُوْهُ
فَلَا يُنَازِعُنَّكَ فِي الْاَمْرِ وَادْعُ اِلٰى
رَبِّكَ ۭ اِنَّكَ لَعَلٰى هُدًى مُّسْتَقِيْمٍ ﴿٦٧﴾

68. Kila umati Tumewajaalia kawaida ya ibada wanayoishikilia, basi wasikugombeze katika jambo hili; na uite kwa Mola wako; bila shaka wewe uko juu ya mwongozo ulio sawa.

Aya 66. Yawezekana kwamba neno *idhini* linahusiana na vimwondo viangukavyo, na sayari zingine za angani ambazo huishambulia ardhi mara kwa mara.

وَاِنْ جٰدَلُوْكَ فَقُلِ اللّٰهُ اَعْلَمُ بِمَا تَعْمَلُوْنَ ﴿٦٩﴾

69. Na kama wakijadiliana nawe, basi sema: Allah Anajua sana mnayoyatenda.

اَللّٰهُ يَحْكُمُ بَيْنَكُمْ يَوْمَ الْقِيٰمَةِ فِيْمَا كُنْتُمْ فِيْهِ تَخْتَلِفُوْنَ ﴿٧٠﴾

70. Allah Atahukumu baina yenu siku ya Kiyama katika yale mliyokuwa mkihitilafiana.

اَلَمْ تَعْلَمْ اَنَّ اللّٰهَ يَعْلَمُ مَا فِي السَّمَآءِ وَالْاَرْضِ ؕ اِنَّ ذٰلِكَ فِيْ كِتٰبٍ ؕ اِنَّ ذٰلِكَ عَلَى اللّٰهِ يَسِيْرٌ ﴿٧١﴾

71. Je, hujui ya kwamba Allah Huyajua yaliyomo mbinguni na ardhini? Bila shaka hayo yamo Kitabuni; hakika hayo kwa Allah ni rahisi.

وَيَعْبُدُوْنَ مِنْ دُوْنِ اللّٰهِ مَا لَمْ يُنَزِّلْ بِهٖ سُلْطٰنًا وَّمَا لَيْسَ لَهُمْ بِهٖ عِلْمٌ ؕ وَمَا لِلظّٰلِمِيْنَ مِنْ نَّصِيْرٍ ﴿٧٢﴾

72. Na wanaabudu kinyume cha Allah ambayo (Allah) Hakuyateremshia dalili, na ambayo kwayo hawana elimu nayo, na wadhalimu hawatakuwa na msaidizi.

وَاِذَا تُتْلٰى عَلَيْهِمْ اٰيٰتُنَا بَيِّنٰتٍ تَعْرِفُ فِيْ وُجُوْهِ الَّذِيْنَ كَفَرُوا الْمُنْكَرَ ؕ يَكَادُوْنَ يَسْطُوْنَ بِالَّذِيْنَ يَتْلُوْنَ عَلَيْهِمْ اٰيٰتِنَا ؕ قُلْ اَفَاُنَبِّئُكُمْ بِشَرٍّ مِّنْ ذٰلِكُمْ ؕ اَلنَّارُ ؕ وَعَدَهَا اللّٰهُ الَّذِيْنَ كَفَرُوْا ؕ وَبِئْسَ الْمَصِيْرُ ﴿٧٣﴾ ع ١٠

73. Na wanaposomewa Aya Zetu zilizo wazi, utaona chuki juu ya nyuso za wale waliokufuru; wapo karibu kuwashambulia wale wanaowasomea Aya Zetu. Sema: Je, niwaambieni yaliyo mabaya zaidi kuliko hayo? Ni Moto Allah Aliowaahidia wale waliokufuru, na ni marudio mabaya.

FUNGU 10

يٰۤاَيُّهَا النَّاسُ ضُرِبَ مَثَلٌ فَاسْتَمِعُوْا لَهٗ ؕ اِنَّ الَّذِيْنَ تَدْعُوْنَ مِنْ دُوْنِ اللّٰهِ لَنْ يَّخْلُقُوْا ذُبَابًا وَّلَوِ اجْتَمَعُوْا لَهٗ ؕ وَاِنْ يَّسْلُبْهُمُ الذُّبَابُ شَيْـًٔا لَّا يَسْتَنْقِذُوْهُ مِنْهُ ؕ ضَعُفَ الطَّالِبُ وَالْمَطْلُوْبُ ﴿٧٤﴾

74. Enyi watu! Imepigwa methali basi mwiisikilize: Hakika wale mnaowaomba badala ya Allah hawawezi kuumba inzi wajapokusanyika kwa jambo hili; na kama inzi akiwanyang'anya cho chote hawawezi kukipokonya kwake. Amedhoofika aombaye na anayeombwa.

Aya 74. Aya hii inadhihirisha unyonge na udhaifu wa miungu ya uwongo kwamba haiwezi kuumba hata nzi; na pia ndani ya Aya hii mna bishara ya kuwa waungu walio dhaifu mwisho wao ni kufutika kabisa, wao pamoja na wafuasi wao. Ndivyo ilivyotokea. Miungu ya masanamu iliyokuwa ndani ya Kaaba yote ilivunjwa na ibada ya masanamu ikaondoka.

مَا قَدَرُوا اللّٰهَ حَقَّ قَدْرِهٖ ؕ اِنَّ اللّٰهَ لَقَوِیٌّ
عَزِیْزٌ ﴿۷۴﴾

75. Hawakumkadiria Allah sawasawa (kwa sifa Zake); hakika Allah bila shaka, ni Mwenye nguvu, Mwenye heshima.

اَللّٰهُ یَصْطَفِیْ مِنَ الْمَلٰٓئِكَةِ رُسُلًا وَّ مِنَ
النَّاسِ ؕ اِنَّ اللّٰهَ سَمِیْعٌۢ بَصِیْرٌ ﴿۷۵﴾ ۚ

76. Allah Huchagua Mitume miongoni mwa Malaika na miongoni mwa watu: Kwa yakini Allah ni Asikiaye, Aonaye.

یَعْلَمُ مَا بَیْنَ اَیْدِیْهِمْ وَ مَا خَلْفَهُمْ ؕ
وَ اِلَی اللّٰهِ تُرْجَعُ الْاُمُوْرُ ﴿۷۶﴾

77. Huyajua yaliyo mbele yao na yaliyo nyuma yao, na kwa Allah ndiko yatarejeshwa mambo.

یٰۤاَیُّهَا الَّذِیْنَ اٰمَنُوا ارْكَعُوْا وَ اسْجُدُوْا
وَ اعْبُدُوْا رَبَّكُمْ وَ افْعَلُوا الْخَیْرَ لَعَلَّكُمْ
تُفْلِحُوْنَ ﴿۷۷﴾ ۩

78. Enyi mlioamini, inameni na sujuduni na Mwabuduni Mola wenu na fanyeni mema, ili mpate kufaulu.

وَ جَاهِدُوْا فِی اللّٰهِ حَقَّ جِهَادِهٖ ؕ هُوَ
اجْتَبٰىكُمْ وَ مَا جَعَلَ عَلَیْكُمْ فِی الدِّیْنِ
مِنْ حَرَجٍ ؕ مِلَّةَ اَبِیْكُمْ اِبْرٰهِیْمَ ؕ هُوَ
سَمّٰىكُمُ الْمُسْلِمِیْنَ ۙ۬ مِنْ قَبْلُ وَ فِیْ هٰذَا
لِیَكُوْنَ الرَّسُوْلُ شَهِیْدًا عَلَیْكُمْ
وَ تَكُوْنُوْا شُهَدَآءَ عَلَی النَّاسِ ۚۖ فَاَقِیْمُوا
الصَّلٰوةَ وَ اٰتُوا الزَّكٰوةَ وَ اعْتَصِمُوْا
بِاللّٰهِ ؕ هُوَ مَوْلٰىكُمْ ۚ فَنِعْمَ الْمَوْلٰی
وَ نِعْمَ النَّصِیْرُ ﴿۷۸﴾ ع

79. Na jitahidini katika (njia ya) Allah jitihada iliyo haki Yake. Yeye Amewachagueni wala Hakuweka juu yenu udhia katika dini, (nayo) ni mila ya baba yenu Ibrahimu; yeye aliwaiteni Waislamu tangu zamani na katika (Qur'an) hii pia, ili awe Mtume shahidi juu yenu na ninyi muwe mashahidi juu ya watu. Kwa hiyo simamisheni Sala na toeni Zaka na shikamaneni na Allah. Yeye ndiye Mola wenu, basi ni Mola Mwema aliyoje, na Msaidizi Mwema aliyoje!

Aya 79. Dini ya kweli ya Mungu ambayo ni dini iliyofuatwa na Mitume wote wa Allah ni Islam, yaani dini ya kujisalimisha kwa Allah. Nabii Ibrahimu aliomba ya kwamba katika wazao wake liweko taifa la Waislamu, yaani, watu waliojisalimisha kwa Allah (sura 2:129); naye mara kwa mara anatajwa katika Qur'an kuwa yu Mwislamu.

Aya hii inamaliza sura hii kwa kuwaambia Waislamu ya kuwa wakiendelea kusimamisha Sala na kutoa Zaka na kushikamana na hukumu za Allah, basi bila shaka Allah atakuwa mlinzi na msaidizi wao, na bila shaka watashinda na kufanikiwa, maana msaada wa Allah na ulinzi Wake ndio kitu bora kisichoweza kushindwa.

سُوْرَةُ الْمُؤْمِنُوْنَ مَكِّيَّةٌ وَّ هِيَ مَعَ الْبَسْمَلَةِ مِائَةٌ وَّ تِسْعَ عَشْرَةَ اٰيَةً وَّ سِتَّةُ رُكُوْعَاتٍ

23. SURA AL-MU'MINUUN

Imeteremshwa Makka

Ina mafungu 6 na Aya 119 pamoja na Bismillahi

JUZU 18

بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ ①

1. Kwa jina la Allah, Mwingi wa rehema, Mwingi wa ukarimu.

قَدْ اَفْلَحَ الْمُؤْمِنُوْنَ ۙ② ع

2. Hakika wamefaulu waaminio.

الَّذِيْنَ هُمْ فِيْ صَلَاتِهِمْ خٰشِعُوْنَ ۙ③

3. Ambao katika Sala zao ni wanyenyekevu.

وَالَّذِيْنَ هُمْ عَنِ اللَّغْوِ مُعْرِضُوْنَ ۙ④

4. Na ambao katika upuuzi ni wajiepushao.

وَالَّذِيْنَ هُمْ لِلزَّكٰوةِ فٰعِلُوْنَ ۙ⑤

5. Na ambao kwa Zaka ni wafanyao (juhudi).

وَالَّذِيْنَ هُمْ لِفُرُوْجِهِمْ حٰفِظُوْنَ ۙ⑥

6. Na ambao kwa tupu zao ni wajilindao.

اِلَّا عَلٰٓى اَزْوَاجِهِمْ اَوْ مَا مَلَكَتْ اَيْمَانُهُمْ فَاِنَّهُمْ غَيْرُ مَلُوْمِيْنَ ۚ⑦

7. Isipokuwa kwa wake zao au kwa (wanawake) wale iliyowamiliki mikono yao ya kuume, basi hakika hao ndio wasiolaumiwa.

فَمَنِ ابْتَغٰى وَرَآءَ ذٰلِكَ فَاُولٰٓئِكَ هُمُ الْعٰدُوْنَ ۚ⑧

8. Lakini anayetaka kinyume cha haya, basi hao ndio warukao mipaka.

وَالَّذِيْنَ هُمْ لِاَمٰنٰتِهِمْ وَعَهْدِهِمْ رٰعُوْنَ ۙ⑨

9. Na ambao kwa amana zao na ahadi zao ni waangaliao.

وَالَّذِيْنَ هُمْ عَلٰى صَلَوٰتِهِمْ يُحَافِظُوْنَ ۘ⑩ ع

10. Na ambao wanazihifadhi sala zao.

Sura hii imeitwa *Waaminio* maana inaeleza mafanikio ya waaminio. Imamu Suyuti anafahamu ya kuwa sura hii ndiyo ya mwisho kushuka Makka.

Aya 3-10. Katika Aya hizi mmeelezwa madaraja sita ya maendeleo ya kiroho ya mwanadamu, daraja baada ya daraja, hata mtu anafikia ukamilifu wa kiroho. Na toka Aya 13-15 yameelezwa madaraja sita ya maendeleo ya kimwili ambayo yanapotimia mtu anakuwa mwanadamu. Katika maendeleo ya dunia mtu hawezi kupata ukamilifu wa kiroho wala wa kimwili mpaka apitie madaraja yote hayo. Elimu hii kwa hakika ni mwujiza wa Qur'an, na hakuna kitabu cho chote kabla ya Qur'an kilichotoa mafundisho ya namna hii. Sasa ni juu ya Waislamu kuangalia, je, hali hizo sita za kiroho zinapatikana kwao? Kama hazipatikani basi wajue hawawezi kufanikiwa,

11. Hao ndio warithi,

اُولٰٓئِكَ هُمُ الْوٰرِثُوْنَ ۙ﴿۱۱﴾

12. Ambao watairithi Pepo; wao humo watakaa.

الَّذِيْنَ يَرِثُوْنَ الْفِرْدَوْسَ ؕ هُمْ فِيْهَا خٰلِدُوْنَ﴿۱۲﴾

13. Na kwa yakini Tulimwumba mwanadamu katika mateuzi ya udongo.

وَلَقَدْ خَلَقْنَا الْاِنْسَانَ مِنْ سُلٰلَةٍ مِّنْ طِيْنٍ ۚ﴿۱۳﴾

14. Kisha Tukamfanya mbegu katika kao lililohifadhika.

ثُمَّ جَعَلْنٰهُ نُطْفَةً فِيْ قَرَارٍ مَّكِيْنٍ ۖ﴿۱۴﴾

15. Kisha Tukaiumba mbegu kuwa pande la damu, na Tukaumba pande la damu kuwa pande la nyama, kisha Tukaumba pande la nyama kuwa mifupa, na mifupa Tukaivika nyama, kisha Tukaifanya kiumbe kingine. Basi mwenye mibaraka ni Allah Mbora wa waumbao.

ثُمَّ خَلَقْنَا النُّطْفَةَ عَلَقَةً فَخَلَقْنَا الْعَلَقَةَ مُضْغَةً فَخَلَقْنَا الْمُضْغَةَ عِظٰمًا فَكَسَوْنَا الْعِظٰمَ لَحْمًا ۗ ثُمَّ اَنْشَاْنٰهُ خَلْقًا اٰخَرَ ؕ فَتَبٰرَكَ اللّٰهُ اَحْسَنُ الْخٰلِقِيْنَ ؕ﴿۱۵﴾

16. Kisha hakika ninyi baada ya hayo ni wenye kufa,

ثُمَّ اِنَّكُمْ بَعْدَ ذٰلِكَ لَمَيِّتُوْنَ ؕ﴿۱۶﴾

17. Kisha hakika ninyi siku ya Kiyama mtafufuliwa.

ثُمَّ اِنَّكُمْ يَوْمَ الْقِيٰمَةِ تُبْعَثُوْنَ ﴿۱۷﴾

18. Na kwa yakini Tuliziumba juu yenu njia saba; nasi katika kuumba si waghafilikao.

وَلَقَدْ خَلَقْنَا فَوْقَكُمْ سَبْعَ طَرَآئِقَ ۖ وَمَا كُنَّا عَنِ الْخَلْقِ غٰفِلِيْنَ﴿۱۸﴾

19. Na Tumeteremsha kutoka mawinguni maji kwa kiasi, na

وَاَنْزَلْنَا مِنَ السَّمَآءِ مَآءًۢ بِقَدَرٍ فَاَسْكَنّٰهُ فِي الْاَرْضِ ۖ وَ اِنَّا عَلٰى ذَهَابٍۭ بِهٖ

maana Allah amekwisha tangaza toka Aya ya mwanzo ya kuwa watakaofanikiwa ni wale wenye kupita madaraja hayo sita, nasi tunaona ya kuwa Waislamu wa zamani waliojali sana mafundisho haya walifanikiwa hadi ya mafanikio.

Aya 15. *Kisha Tukaifanya kiumbe kingine.* Maneno haya yanaonyesha ya kwamba mtu anapoendelea kuumbika katika mwili, roho yake pia inaendelea kuumbika mpaka mwili unakuwa kamili na roho pia inajitokeza, ndipo kiumbe anakuwa mtu kamili. Katika fundisho hili mna hekima nyingine ya kuwa mtu anapotimia maneno yake na matendo yake kwa kumtukuza Allah, nayo yanatunga roho na inajitokeza katika ukamilifu wa tabia kama vile roho inavyojitokeza katika mwili wa binadamu na anakuwa mtu kamili.

Aya 16-17. Aya hizi zinaonyesha ya kwamba mara mtu anapokufa na kuonja maisha ya Akhera, hawezi tena kurudishwa duniani ila atafufuliwa huko huko kukutana na Kiyama kikubwa.

Aya 19. *Sisi kwa kuyaondoa ni Wawezao.* Jambo hili linaonekana kila mara. Mwenyezi

Tukayatuliza ardhini, na bila shaka Sisi Tunao uwezo wa kuyaondoa.

لَقٰدِرُوْنَ ﴿١٨﴾

20. Kisha kwa hayo Tukawafanyieni bustani za mitende na mizabibu; mnapata humo matunda mengi, na katika hayo mnakula.

فَاَنْشَاْنَا لَكُمْ بِهٖ جَنّٰتٍ مِّنْ نَّخِيْلٍ وَّاَعْنَابٍ ۖ لَكُمْ فِيْهَا فَوَاكِهُ كَثِيْرَةٌ وَّمِنْهَا تَاْكُلُوْنَ ﴿٢٠﴾

21. Na mti utokao katika mlima wa Sinai; unatoa mafuta na viungo vingi kwa walao.

وَشَجَرَةً تَخْرُجُ مِنْ طُوْرِ سَيْنَآءَ تَنْۢبُتُ بِالدُّهْنِ وَصِبْغٍ لِّلْاٰكِلِيْنَ ﴿٢١﴾

22. Na hakika mnalo fundisho katika wanyama: Tunawanywesheni katika vile vilivyomo matumboni mwao, na mnapata katika hao manufaa mengi, na katika hao mnakula.

وَاِنَّ لَكُمْ فِى الْاَنْعَامِ لَعِبْرَةً ۖ نُسْقِيْكُمْ مِّمَّا فِىْ بُطُوْنِهَا وَلَكُمْ فِيْهَا مَنَافِعُ كَثِيْرَةٌ وَّمِنْهَا تَاْكُلُوْنَ ﴿٢٢﴾

23. Na juu yao na juu ya merikebu mnabebwa.

وَعَلَيْهَا وَعَلَى الْفُلْكِ تُحْمَلُوْنَ ﴿٢٣﴾

FUNGU 2

24. Na bila shaka Tulimtuma Nuhu kwa watu wake, na akasema: Enyi watu wangu, Mwabuduni Allah, hamna mungu isipokuwa Yeye; basi je, hamwogopi?

وَلَقَدْ اَرْسَلْنَا نُوْحًا اِلٰى قَوْمِهٖ فَقَالَ يٰقَوْمِ اعْبُدُوا اللّٰهَ مَا لَكُمْ مِّنْ اِلٰهٍ غَيْرُهٗ ۖ اَفَلَا تَتَّقُوْنَ ﴿٢٤﴾

25. Lakini wakasema wakuu wa wale waliokufuru katika watu wake: Siye huyu ila ni mtu kama ninyi, anataka kujipatia ubora juu yenu; na kama Allah Angependa, kwa yakini Angeliteremsha Malaika. Hatukusikia haya kwa baba zetu wa kwanza.

فَقَالَ الْمَلَؤُا الَّذِيْنَ كَفَرُوْا مِنْ قَوْمِهٖ مَا هٰذَآ اِلَّا بَشَرٌ مِّثْلُكُمْ ۙ يُرِيْدُ اَنْ يَّتَفَضَّلَ عَلَيْكُمْ ۭ وَلَوْ شَآءَ اللّٰهُ لَاَنْزَلَ مَلٰٓئِكَةً ۚ مَّا سَمِعْنَا بِهٰذَا فِىْٓ اٰبَآئِنَا الْاَوَّلِيْنَ ﴿٢٥﴾

Mungu huteremsha mvua, maji yakakaa ardhini, kisha yakapanda tena mbinguni katika sura ya mvuke. Namna hii maji ya kiroho, yaani wahyi, hushuka duniani ukakaa muda na kuleta faida, kisha unazuiliwa, na kisha unaletwa tena kama vile nyakati za mvua na za jua zinavyopishana.

Aya 25. *Ni mtu kama ninyi.* Fikira hii ndiyo inayowakosesha watu wengi kupata faida na kushika haki. Mtu hufikiri mbona nikajifunze kwa fulani na hali yeye ni mtu kama mimi. Kadhalika ingawa watu wanajua habari za Manabii mamia na mamia waliopita ambao walikuwa watu kama wao, juu ya hayo anapofika Nabii hawataki kumkubali wakisema ati naye ni mtu tu kama wao. Fikira ya namna hii imewakosesha watu heri nyingi.

اِنۡ هُوَ اِلَّا رَجُلٌۢ بِهٖ جِنَّةٌ فَتَرَبَّصُوۡا بِهٖ حَتّٰى حِيۡنٍ ﴿۲۶﴾

26. Huyu siye ila ni mtu mwenye wazimu, basi mngojeeni kwa muda.

قَالَ رَبِّ انۡصُرۡنِىۡ بِمَا كَذَّبُوۡنِ ﴿۲۷﴾

27. (Nuhu) akasema: Mola wangu, Unisaidie kwa sababu wamenikadhibisha.

فَاَوۡحَيۡنَاۤ اِلَيۡهِ اَنِ اصۡنَعِ الۡفُلۡكَ بِاَعۡيُنِنَا وَوَحۡيِنَا فَاِذَا جَآءَ اَمۡرُنَا وَفَارَ التَّنُّوۡرُ ۙ فَاسۡلُكۡ فِيۡهَا مِنۡ كُلٍّ زَوۡجَيۡنِ اثۡنَيۡنِ وَاَهۡلَكَ اِلَّا مَنۡ سَبَقَ عَلَيۡهِ الۡقَوۡلُ مِنۡهُمۡ‌ۚ وَلَا تُخَاطِبۡنِىۡ فِى الَّذِيۡنَ ظَلَمُوۡا‌ۚ اِنَّهُمۡ مُّغۡرَقُوۡنَ ﴿۲۸﴾

28. Basi Tulimfunulia ya kwamba: unda safina mbele ya macho Yetu na (sawa na) ufunuo Wetu. Basi itakapofika amri Yetu na bonde kufurika, hapo uwaingize ndani yake wawili wa kila namna, na ahali zako, ila ambaye kauli imepita juu yake miongoni mwao. Wala usinizungumze juu ya wale waliodhulumu, bila shaka wao watagharikishwa.

فَاِذَا اسۡتَوَيۡتَ اَنۡتَ وَمَنۡ مَّعَكَ عَلَى الۡفُلۡكِ فَقُلِ الۡحَمۡدُ لِلّٰهِ الَّذِىۡ نَجّٰٮنَا مِنَ الۡقَوۡمِ الظّٰلِمِيۡنَ ﴿۲۹﴾

29. Na utakapotulia, wewe na walio pamoja nawe, merikebuni, basi sema: Sifa zote njema ni za Allah Ambaye Ametuokoa katika watu wadhalimu.

وَقُلۡ رَّبِّ اَنۡزِلۡنِىۡ مُنۡزَلًا مُّبٰرَكًا وَّاَنۡتَ خَيۡرُ الۡمُنۡزِلِيۡنَ ﴿۳۰﴾

30. Na sema: Mola wangu, Uniteremshe mteremsho wenye baraka, maana Wewe ni Mbora wa wateremshao.

اِنَّ فِىۡ ذٰلِكَ لَاٰيٰتٍ وَّاِنۡ كُنَّا لَمُبۡتَلِيۡنَ ﴿۳۱﴾

31. Bila shaka katika hayo zimo Ishara, na kwa yakini Sisi Tulikuwa Tunaojaribu (watu).

ثُمَّ اَنۡشَاۡنَا مِنۡۢ بَعۡدِهِمۡ قَرۡنًا اٰخَرِيۡنَ ﴿۳۲﴾

32. Kisha Tuliumba baada yao kizazi kingine.

Aya 28. *Unda safina mbele ya macho Yetu na (sawa na) ufunuo Wetu.* Safina ndogo, lakini imeundwa kwa amri ya Allah, imeweza kuwaletea watu faida na kuwaokoa katika gharika yenye tufani kubwa. Hivi ndivyo yalivyo maajabu ya Allah. Cho chote kinachofanyika kwa amri ya Allah na kiwe kidogo namna gani au kionekane machoni pa watu kuwa cha upuuzi, lakini lazima kitaleta manufaa.

Aya 30. Aya hii inatufundisha somo la maana sana. Mara nyingi mtu akipona ndani ya taabu, basi hana haja tena ya kuomba salama kwa Allah. Hapa tunaambiwa ya kuwa kuomba baraka baada ya kupona katika hatari ndio mwendo mwema unaotakiwa na Allah.

فَاَرْسَلْنَا فِيْهِمْ رَسُوْلًا مِّنْهُمْ اَنِ اعْبُدُوا اللّٰهَ مَا لَكُمْ مِّنْ اِلٰهٍ غَيْرُهٗ ؕ اَفَلَا تَتَّقُوْنَ ﴿۳۳﴾ ع ۲

33. Na Tukawapelekea Mtume kutoka miongoni mwao, kuwaambia: Mwabuduni Allah, hamna Mungu isipokuwa Yeye; je, hamwogopi?

FUNGU 3

وَقَالَ الْمَلَاُ مِنْ قَوْمِهِ الَّذِيْنَ كَفَرُوْا وَكَذَّبُوْا بِلِقَآءِ الْاٰخِرَةِ وَاَتْرَفْنٰهُمْ فِى الْحَيٰوةِ الدُّنْيَا ۙ مَا هٰذَآ اِلَّا بَشَرٌ مِّثْلُكُمْ ۙ يَاْكُلُ مِمَّا تَاْكُلُوْنَ مِنْهُ وَيَشْرَبُ مِمَّا تَشْرَبُوْنَ ﴿۳۴﴾

34. Na wakasema wakubwa katika watu wake waliokufuru na kukadhibisha mkutano wa Akhera, na Tuliowatajirisha katika maisha ya dunia: Huyu siye ila ni mtu kama ninyi, anakula katika vile mnavyokula na anakunywa katika vile mnavyokunywa.

وَلَئِنْ اَطَعْتُمْ بَشَرًا مِّثْلَكُمْ اِنَّكُمْ اِذًا لَّخٰسِرُوْنَ ﴿۳۵﴾

35. Na kama mkimtii mtu kama ninyi, kwa hakika hapo mtakuwa wapatao hasara.

اَيَعِدُكُمْ اَنَّكُمْ اِذَا مِتُّمْ وَكُنْتُمْ تُرَابًا وَّعِظَامًا اَنَّكُمْ مُّخْرَجُوْنَ ﴿۳۶﴾

36. Je! anawatishieni ya kwamba mtakapokufa na kuwa udongo na mifupa, hakika mtatolewa?

هَيْهَاتَ هَيْهَاتَ لِمَا تُوْعَدُوْنَ ﴿۳۷﴾

37. Hayawi! Hayawi! hayo mnayoahidiwa.

اِنْ هِىَ اِلَّا حَيَاتُنَا الدُّنْيَا نَمُوْتُ وَنَحْيَا وَمَا نَحْنُ بِمَبْعُوْثِيْنَ ﴿۳۸﴾

38. Ni hapa hapa tu ndipo tunapoishi maisha yetu. Tunakufa hapa hapa na tunaishi hapa hapa, na kamwe hatutafufuliwa tena.

اِنْ هُوَ اِلَّا رَجُلٌ افْتَرٰى عَلَى اللّٰهِ كَذِبًا وَّمَا نَحْنُ لَهٗ بِمُؤْمِنِيْنَ ﴿۳۹﴾

39. Huyu siye ila ni mtu aliyetunga juu ya Allah uwongo, wala sisi si wenye kumwamini.

قَالَ رَبِّ انْصُرْنِىْ بِمَا كَذَّبُوْنِ ﴿۴۰﴾

40. Akasema: Mola wangu, nisaidie kwa sababu wamenikadhibisha.

قَالَ عَمَّا قَلِيْلٍ لَّيُصْبِحُنَّ نٰدِمِيْنَ ﴿۴۱﴾ ج

41. Akasema: Bado kidogo, kwa yakini watakuwa wajutao.

Aya 40. *Mola wangu, nisaidie.* Kuomba kwa Allah ndiyo silaha waliyokuwa wakiitumia Manabii wa Allah, nayo ndiyo silaha yenye nguvu, iliyowapitisha salama katika kila hatari.

فَاَخَذَتْهُمُ الصَّيْحَةُ بِالْحَقِّ فَجَعَلْنٰهُمْ غُثَآءً ۚ فَبُعْدًا لِّلْقَوْمِ الظّٰلِمِيْنَ ﴿٤٢﴾

42. Basi ikawashika adhabu kwa haki na Tukawafanya kuwa takataka; basi maangamio kwa watu wadhalimu.

ثُمَّ اَنْشَاْنَا مِنْۢ بَعْدِهِمْ قُرُوْنًا اٰخَرِيْنَ ﴿٤٣﴾

43. Kisha Tukaviumba baada yao vizazi vingine.

مَا تَسْبِقُ مِنْ اُمَّةٍ اَجَلَهَا وَمَا يَسْتَاْخِرُوْنَ ﴿٤٤﴾

44. Hakuna umati uwezao kuutanguliza muda wake ulioahidiwa wala kukawiza.

ثُمَّ اَرْسَلْنَا رُسُلَنَا تَتْرَا ؕ كُلَّمَا جَآءَ اُمَّةً رَّسُوْلُهَا كَذَّبُوْهُ فَاَتْبَعْنَا بَعْضَهُمْ بَعْضًا وَّجَعَلْنٰهُمْ اَحَادِيْثَ ۚ فَبُعْدًا لِّقَوْمٍ لَّا يُؤْمِنُوْنَ ﴿٤٥﴾

45. Kisha Tukawatuma Mitume Wetu, mmoja baada ya mmoja; kila mara alipowafikia watu Mtume wao walimkadhibisha; hivyo Tukawafuatanisha baadhi yao kwa wengine, na Tukawafanya kuwa visa; basi maangamio kwa watu wasioamini.

ثُمَّ اَرْسَلْنَا مُوْسٰى وَاَخَاهُ هٰرُوْنَ ۙ بِاٰيٰتِنَا وَسُلْطٰنٍ مُّبِيْنٍ ۙ﴿٤٦﴾

46. Kisha Tulimtuma Musa na nduguye Harun pamoja na Ishara Zetu na dalili dhahiri.

اِلٰى فِرْعَوْنَ وَمَلَا۟ئِهٖ فَاسْتَكْبَرُوْا وَكَانُوْا قَوْمًا عَالِيْنَ ﴿٤٧﴾ۚ

47. Kwa Firauni na wakuu wake, lakini wakajivuna, nao walikuwa watu wajeuri.

فَقَالُوْٓا اَنُؤْمِنُ لِبَشَرَيْنِ مِثْلِنَا وَقَوْمُهُمَا لَنَا عٰبِدُوْنَ ﴿٤٨﴾ۚ

48. Na wakasema: Je, tuwaamini watu wawili walio mfano wetu na watu wao ni watumwa wetu?

فَكَذَّبُوْهُمَا فَكَانُوْا مِنَ الْمُهْلَكِيْنَ ﴿٤٩﴾

49. Basi wakawakadhibisha na wakawa miongoni mwa walioangamizwa.

وَلَقَدْ اٰتَيْنَا مُوْسَى الْكِتٰبَ لَعَلَّهُمْ يَهْتَدُوْنَ ﴿٥٠﴾

50. Na bila shaka Tulimpa Musa Kitabu ili wapate kuongoka.

وَجَعَلْنَا ابْنَ مَرْيَمَ وَاُمَّهٗٓ اٰيَةً وَّاٰوَيْنٰهُمَآ اِلٰى رَبْوَةٍ ذَاتِ قَرَارٍ وَّمَعِيْنٍ ﴿٥١﴾ ع ٣

51. Na Tulimfanya mwana wa Mariamu na mama Yake kuwa Ishara, na Tukawapa makimbilio kwenye mahali palipoinuka penye starehe na chemchem.

Aya 45. Hapa Allah ameeleza desturi Yake nyingine, ya kuwa, baada ya kuleta Sheria anaipelekea Mitume wa kuisaidia, na Kitabu cha Biblia ni shahidi juu ya jambo hili ya kuwa hata katika wakati mmoja waliweza kuwako Manabii wengi.

Aya 51. *Aya,* "Ishara." Neno hili pia lina maana ya "mfano mwema."

FUNGU 4

يٰٓاَيُّهَا الرُّسُلُ كُلُوْا مِنَ الطَّيِّبٰتِ وَاعْمَلُوْا صَالِحًا ؕ اِنِّيْ بِمَا تَعْمَلُوْنَ عَلِيْمٌ ﴿٥١﴾

52. Enyi Mitume! kuleni katika vitu vizuri na fanyeni mema, hakika Mimi ni Mjuzi wa (hayo) mnayoyatenda.

وَاِنَّ هٰذِهٖٓ اُمَّتُكُمْ اُمَّةً وَّاحِدَةً وَّاَنَا رَبُّكُمْ فَاتَّقُوْنِ ﴿٥٢﴾

53. Na kwa yakini huu umati wenu ni umati mmoja, na Mimi ni Mola wenu, basi Niogopeni.

فَتَقَطَّعُوْٓا اَمْرَهُمْ بَيْنَهُمْ زُبُرًا ؕ كُلُّ حِزْبٍۭ بِمَا لَدَيْهِمْ فَرِحُوْنَ ﴿٥٣﴾

54. Lakini wamekata jambo lao baina yao sehemu-sehemu, kila kundi likifurahia waliyo nayo.

فَذَرْهُمْ فِيْ غَمْرَتِهِمْ حَتّٰى حِيْنٍ ﴿٥٤﴾

55. Basi waache katika ujinga wao hadi muda (fulani).

اَيَحْسَبُوْنَ اَنَّمَا نُمِدُّهُمْ بِهٖ مِنْ مَّالٍ وَّبَنِيْنَ ﴿٥٥﴾ۙ

56. Je, wanafikiri ya kuwa Tunawasaidia kwa mali na watoto,

نُسَارِعُ لَهُمْ فِي الْخَيْرٰتِ ؕ بَلْ لَّا يَشْعُرُوْنَ ﴿٥٦﴾

57. Tunawaharakishia katika mambo ya heri? Bali hawatambui.

اِنَّ الَّذِيْنَ هُمْ مِّنْ خَشْيَةِ رَبِّهِمْ مُّشْفِقُوْنَ ﴿٥٧﴾ۙ

58. Kwa hakika, wale waiogopao haiba ya Mola wao.

وَالَّذِيْنَ هُمْ بِاٰيٰتِ رَبِّهِمْ يُؤْمِنُوْنَ ﴿٥٨﴾ۙ

59. Na ambao huziamini aya za Mola wao.

Aawaa. Neno hili katika lugha ya Kiarabu hutumika kwa ajili ya salama inayopatikana baada ya shida na mashaka makubwa na udhia mwingi. Katika habari za maisha ya Nabii Isa na mama yake, hakuna tukio lo lote jingine la taabu waliyopata isipokuwa taabu ile tu ya kupigiliwa msalabani. Hivyo, kimbilio hili linalosemwa hapa ni lile walilopata baada ya kupigiliwa Yesu msalabani. Mahali walipokimbilia pametajwa katika Aya hii kwa sifa tatu: (1) *Rabwah,* (palipoinuka); (2) *dhaata qaraarin* (penye starehe); (3) *wa ma'iin* (na penye chemchem). Nchi ya Kashmir inapatana kabisa na maelezo haya, hata watu wameipanga jina kuwa ni "pepo ya duniani."

Kama tujuavyo Nabii Isa alitumwa kwa Waisraeli, na nchi hii ya Kashmir imekaliwa toka miaka mingi na Waisraeli waliofunguliwa katika utumwa wa Babili. Jinsi nchi hii ilivyofanana na nchi yao ya asili wameiita jina la *Ka-Ashir* (Kashmir) ambalo maana yake ni "Kama Syria." Tabia za watu hao na umbo lao ni sawa na Mayahudi, na hata baadhi ya majina ya miji ya Kashmir ni yale ya miji yao ya Syria ya zamani. Kwa watu hawa ndiko alikokimbilia Nabii Isa na mama yake baada ya taabu ya kupigiliwa msalabani. Jambo hili katika uchunguzi wa kisasa limehakikishwa kuwa Yesu Kristo alikimbilia Kashmir pamoja na mama yake, na hata kaburi lake liko huko katika mji wa Srinagar, mtaa wa Khanyar.

Aya 52. Aya hii inaonyesha ya kuwa mtu huweza kutenda mema akila vyakula vizuri. Neno *tayyib* maana yake ni kitu halali tena kizuri. Kitu kilichooza si *tayyib.* Dini ya Kiislamu inataka watu watumie vitu vinavyoweza kuwaletea utakaso wa moyo na kuwapa afya njema.

60. Na ambao hawamshirikishi Mola wao.

61. Na ambao wanatoa waliyopewa hali mioyo yao inaogopa kwamba watarejea kwa Mola wao,

62. Hao ndio wafanyao haraka katika mambo ya heri, nao ni wapitao mbele kwa hayo.

63. Nasi Hatuikalifishi nafsi ila kwa wasaa wake, na Tunacho kitabu kisemacho kweli, nao hawatadhulumiwa.

64. Lakini mioyo imo katika ujinga kwa hayo na wanavyo vitendo ghairi ya hivyo wanavyovitenda.

65. Hata Tutakapowashika matajiri wao kwa adhabu, ndipo watalalama.

66. Msilalame leo; bila shaka ninyi hamtasaidiwa nasi.

67. Hakika zilikuwa Aya Zangu zikisomwa kwenu, lakini mlikuwa kwa visigino vyenu mkirudi nyuma,

68. Mkitakabari, mkiizungumza usiku kwa dharau.

69. Je, hawakuitafakari kauli? au yamewafikia yasiyowafikia baba zao wa kwanza?

70. Au hawakumtambua Mtume wao na hivyo ni wamkataao?

71. Au wanasema: (Huyu) ni mwenye wazimu? Bali amewafikia kwa haki, na wengi wao haki ni waichukiao.

وَالَّذِيْنَ هُمْ بِرَبِّهِمْ لَا يُشْرِكُوْنَ ﴿٦٠﴾
وَالَّذِيْنَ يُؤْتُوْنَ مَآ اٰتَوْا وَّقُلُوْبُهُمْ وَجِلَةٌ
اَنَّهُمْ اِلٰى رَبِّهِمْ رٰجِعُوْنَ ﴿٦١﴾
اُولٰٓئِكَ يُسٰرِعُوْنَ فِي الْخَيْرٰتِ وَهُمْ لَهَا
سٰبِقُوْنَ ﴿٦٢﴾
وَلَا نُكَلِّفُ نَفْسًا اِلَّا وُسْعَهَا وَلَدَيْنَا
كِتٰبٌ يَّنْطِقُ بِالْحَقِّ وَهُمْ لَا يُظْلَمُوْنَ ﴿٦٣﴾
بَلْ قُلُوْبُهُمْ فِيْ غَمْرَةٍ مِّنْ هٰذَا وَلَهُمْ
اَعْمَالٌ مِّنْ دُوْنِ ذٰلِكَ هُمْ لَهَا عٰمِلُوْنَ ﴿٦٤﴾
حَتّٰٓى اِذَآ اَخَذْنَا مُتْرَفِيْهِمْ بِالْعَذَابِ
اِذَا هُمْ يَجْـَٔرُوْنَ ﴿٦٥﴾
لَا تَجْـَٔرُوا الْيَوْمَ ۖ اِنَّكُمْ مِّنَّا لَا تُنْصَرُوْنَ ﴿٦٦﴾
قَدْ كَانَتْ اٰيٰتِيْ تُتْلٰى عَلَيْكُمْ فَكُنْتُمْ عَلٰٓى
اَعْقَابِكُمْ تَنْكِصُوْنَ ﴿٦٧﴾
مُسْتَكْبِرِيْنَ ۖ بِهٖ سٰمِرًا تَهْجُرُوْنَ ﴿٦٨﴾
اَفَلَمْ يَدَّبَّرُوا الْقَوْلَ اَمْ جَآءَهُمْ مَّا
لَمْ يَاْتِ اٰبَآءَهُمُ الْاَوَّلِيْنَ ﴿٦٩﴾
اَمْ لَمْ يَعْرِفُوْا رَسُوْلَهُمْ فَهُمْ لَهٗ
مُنْكِرُوْنَ ﴿٧٠﴾
اَمْ يَقُوْلُوْنَ بِهٖ جِنَّةٌ ۭ بَلْ جَآءَهُمْ بِالْحَقِّ
وَاَكْثَرُهُمْ لِلْحَقِّ كٰرِهُوْنَ ﴿٧١﴾

Aya 61. *Hali mioyo yao inaogopa.* Mradi wake ni mioyo kuogopa, je, matendo yangu mema nitendayo yanakubaliwa au hayakubaliwi na Allah? Bibi Aisha alimwuliza Mtume *s.a.w.,* Mtu anazini na anakwiba na hali moyo wake unaogopa, je, ataokoka? Mtume s.a.w. akajibu, La. Ewe binti Siddik, afanye vitendo vizuri na kisha aogope, je, vitakubaliwa au hapana?

وَلَوِ اتَّبَعَ الْحَقُّ اَهْوَآءَهُمْ لَفَسَدَتِ
السَّمٰوٰتُ وَالْاَرْضُ وَمَنْ فِيْهِنَّ ؕ بَلْ
اَتَيْنٰهُمْ بِذِكْرِهِمْ فَهُمْ عَنْ ذِكْرِهِمْ
مُّعْرِضُوْنَ ﴿٧٢﴾

72. Na kama haki ingalifuata matamanio yao, zingaliharibika mbingu na ardhi na vilivyomo humo. Bali, Tumewaletea ukumbusho wao, lakini wanajitenga mbali na ukumbusho wao.

اَمْ تَسْـَٔلُهُمْ خَرْجًا فَخَرَاجُ رَبِّكَ خَيْرٌ ۖ
وَّهُوَ خَيْرُ الرّٰزِقِيْنَ ﴿٧٣﴾

73. Au unawaomba ujira? Lakini ujira wa Mola wako ni bora, naye ni Mbora wa wanaoruzuku.

وَاِنَّكَ لَتَدْعُوْهُمْ اِلٰى صِرَاطٍ
مُّسْتَقِيْمٍ ﴿٧٤﴾

74. Na kwa yakini wewe unawaita kwenye njia iliyonyoka.

وَاِنَّ الَّذِيْنَ لَا يُؤْمِنُوْنَ بِالْاٰخِرَةِ عَنِ
الصِّرَاطِ لَنٰكِبُوْنَ ﴿٧٥﴾

75. Na hakika wale wasioiamini Akhera bila shaka ndio wajitengao mbali na njia iliyonyooka.

وَلَوْ رَحِمْنٰهُمْ وَكَشَفْنَا مَا بِهِمْ مِّنْ
ضُرٍّ لَّلَجُّوْا فِيْ طُغْيَانِهِمْ يَعْمَهُوْنَ ﴿٧٦﴾

76. Na Tukiwarehemu na kuwaondolea shida waliyo nayo bila shaka wataendelea katika upotevu wao wakihangaika.

وَلَقَدْ اَخَذْنٰهُمْ بِالْعَذَابِ فَمَا اسْتَكَانُوْا
لِرَبِّهِمْ وَمَا يَتَضَرَّعُوْنَ ﴿٧٧﴾

77. Na hakika Tuliwashika kwa adhabu, lakini hawakuelekea kwa Mola wao wala hawakunyenyekea.

حَتّٰۤى اِذَا فَتَحْنَا عَلَيْهِمْ بَابًا ذَا عَذَابٍ
شَدِيْدٍ اِذَا هُمْ فِيْهِ مُبْلِسُوْنَ ﴿٧٨﴾ ع ٤

78. Mpaka Tulipowafungulia mlango wa adhabu kali, ndipo wakawa wenye kukata tamaa.

FUNGU 5

وَهُوَ الَّذِيْۤ اَنْشَاَ لَكُمُ السَّمْعَ وَالْاَبْصَارَ
وَالْاَفْـِٕدَةَ ؕ قَلِيْلًا مَّا تَشْكُرُوْنَ ﴿٧٩﴾

79. Na Yeye ndiye Aliyewaumbieni masikio na macho na mioyo: ni kidogo mnayoyashukuru.

وَهُوَ الَّذِيْ ذَرَاَكُمْ فِي الْاَرْضِ وَاِلَيْهِ
تُحْشَرُوْنَ ﴿٨٠﴾

80. Naye ndiye Aliyewaenezeni katika ardhi, na Kwake mtakusanywa.

وَهُوَ الَّذِيْ يُحْيٖ وَيُمِيْتُ وَلَهُ اخْتِلَافُ
الَّيْلِ وَالنَّهَارِ ؕ اَفَلَا تَعْقِلُوْنَ ﴿٨١﴾

81. Na Yeye ndiye Anahuisha na kufisha, na ni Yake mabadiliko ya usiku na mchana; basi je, hamfahamu?

Aya 81. *Mabadiliko ya usiku na mchana* pia mradi wake ni kuwa huku wakiwa na mchana, upande mwingine wanakuwa na usiku, na huku wanapokuwa na usiku wengine upande mwingine wanakuwa na mchana.

بَلْ قَالُوْا مِثْلَ مَا قَالَ الْاَوَّلُوْنَ ﴿٨٢﴾

82. Bali wakasema kama walivyosema (watu) wa awali.

قَالُوْٓا ءَاِذَا مِتْنَا وَكُنَّا تُرَابًا وَّعِظَامًا ءَاِنَّا لَمَبْعُوْثُوْنَ ﴿٨٣﴾

83. Walikuwa wakisema: Je, Tutakapokufa na kuwa udongo na mifupa, je, tutafufuliwa?

لَقَدْ وُعِدْنَا نَحْنُ وَاٰبَآؤُنَا هٰذَا مِنْ قَبْلُ اِنْ هٰذَآ اِلَّآ اَسَاطِيْرُ الْاَوَّلِيْنَ ﴿٨٤﴾

84. Bila shaka tuliahidiwa haya sisi na baba zetu zamani: haya siyo ila visa vya (watu) wa kwanza.

قُلْ لِّمَنِ الْاَرْضُ وَمَنْ فِيْهَآ اِنْ كُنْتُمْ تَعْلَمُوْنَ ﴿٨٥﴾

85. Sema: Ni ya nani ardhi na vilivyomo kama ninyi mnajua?

سَيَقُوْلُوْنَ لِلّٰهِ ؕ قُلْ اَفَلَا تَذَكَّرُوْنَ ﴿٨٦﴾

86. Watasema: Ni ya Allah! Sema: Basi je, hamshiki nasaha?

قُلْ مَنْ رَّبُّ السَّمٰوٰتِ السَّبْعِ وَرَبُّ الْعَرْشِ الْعَظِيْمِ ﴿٨٧﴾

87. Sema: Ni nani Mola wa mbingu saba na Mola wa Arshi kuu.

سَيَقُوْلُوْنَ لِلّٰهِ ؕ قُلْ اَفَلَا تَتَّقُوْنَ ﴿٨٨﴾

88. Watasema: Ni vya Allah. Sema: Basi je, hamwogopi?

قُلْ مَنْۢ بِيَدِهٖ مَلَكُوْتُ كُلِّ شَيْءٍ وَّهُوَ يُجِيْرُ وَلَا يُجَارُ عَلَيْهِ اِنْ كُنْتُمْ تَعْلَمُوْنَ ﴿٨٩﴾

89. Sema: Ni nani mkononi Mwake umo ufalme wa kila kitu, naye ndiye Alindaye na (mtu) halindwi kinyume naye, kama mnajua?

سَيَقُوْلُوْنَ لِلّٰهِ ؕ قُلْ فَاَنّٰى تُسْحَرُوْنَ ﴿٩٠﴾

90. Watasema: Ni wa Allah. Sema: Basi vipi mnadanganywa?

بَلْ اَتَيْنٰهُمْ بِالْحَقِّ وَاِنَّهُمْ لَكٰذِبُوْنَ ﴿٩١﴾

91. Bali Tumewaletea haki, na kwa yakini hao ndio waongo.

مَا اتَّخَذَ اللّٰهُ مِنْ وَّلَدٍ وَّمَا كَانَ مَعَهٗ مِنْ اِلٰهٍ ۚ اِذًا لَّذَهَبَ كُلُّ اِلٰهٍۢ بِمَا خَلَقَ وَلَعَلَا بَعْضُهُمْ عَلٰى بَعْضٍ ؕ سُبْحٰنَ اللّٰهِ عَمَّا يَصِفُوْنَ ﴿٩٢﴾

92. Allah Hakujishikia mwana wala hakuwa pamoja naye mungu mwingine, hapo kila mungu angaliwachukua aliowaumba, na baadhi yao wangali washinda wengine; Allah ni Mtakatifu, Ameepukana na sifa wanazomsifu.

عٰلِمِ الْغَيْبِ وَالشَّهَادَةِ فَتَعٰلٰى عَمَّا يُشْرِكُوْنَ ﴿٩٣﴾ ع

93. Mjuzi wa siri na dhahiri, na Aliye juu kuliko wanayoyashirikisha.

FUNGU 6

قُلْ رَّبِّ اِمَّا تُرِيَنِّيْ مَا يُوْعَدُوْنَ ﴿٩٤﴾

94. Sema: Mola wangu! Ukinionyesha waliyoyaahidiwa:

رَبِّ فَلَا تَجْعَلْنِيْ فِي الْقَوْمِ الظّٰلِمِيْنَ ﴿٩٥﴾

95. Mola wangu! Usinijaalie kuwa miongoni mwa watu wadhalimu.

وَاِنَّا عَلٰٓى اَنْ نُّرِيَكَ مَا نَعِدُهُمْ لَقٰدِرُوْنَ ﴿٩٦﴾

96. Na hakika sisi kwa kukuonyesha Tuliyowaahidi ni Wawezao.

اِدْفَعْ بِالَّتِيْ هِيَ اَحْسَنُ السَّيِّئَةَ ؕ نَحْنُ اَعْلَمُ بِمَا يَصِفُوْنَ ﴿٩٧﴾

97. Uzuie ubaya kwa yaliyo bora; Sisi Tunajua wanayoyaeleza.

وَقُلْ رَّبِّ اَعُوْذُبِكَ مِنْ هَمَزٰتِ الشَّيٰطِيْنِ ﴿٩٨﴾

98. Na sema: Mola wangu! najikinga Kwako (Uniepushe) na wasiwasi wa mashetani,

وَاَعُوْذُبِكَ رَبِّ اَنْ يَّحْضُرُوْنِ ﴿٩٩﴾

99. Na najikinga Kwako, Mola wangu, ili wasinihudhurie.

حَتّٰٓى اِذَا جَآءَ اَحَدَهُمُ الْمَوْتُ قَالَ رَبِّ ارْجِعُوْنِ ﴿١٠٠﴾

100. Hata yanapomfikia mmoja wao mauti, husema: Mola wangu, Unirudishe:

لَعَلِّيْٓ اَعْمَلُ صَالِحًا فِيْمَا تَرَكْتُ كَلَّا ؕ اِنَّهَا كَلِمَةٌ هُوَ قَآئِلُهَا ؕ وَمِنْ وَّرَآئِهِمْ بَرْزَخٌ اِلٰى يَوْمِ يُبْعَثُوْنَ ﴿١٠١﴾

101. Ili nifanye mema katika yale niliyoyaacha. Hapana! Hakika hili ni neno tu analolisema; na nyuma yao iko kinga mpaka siku watakapofufuliwa.

فَاِذَا نُفِخَ فِي الصُّوْرِ فَلَآ اَنْسَابَ بَيْنَهُمْ يَوْمَئِذٍ وَّلَا يَتَسَآءَلُوْنَ ﴿١٠٢﴾

102. Basi litakapopulizwa parapanda, hapo hautakuwapo ujamaa baina yao siku hiyo, wala hawataulizana.

فَمَنْ ثَقُلَتْ مَوَازِيْنُهٗ فَاُولٰٓئِكَ هُمُ الْمُفْلِحُوْنَ ﴿١٠٣﴾

103. Kisha wale ambao mizani yao (ya matendo) itakuwa mizito, basi hao ndio wenye kufaulu.

وَمَنْ خَفَّتْ مَوَازِيْنُهٗ فَاُولٰٓئِكَ الَّذِيْنَ خَسِرُوْٓا اَنْفُسَهُمْ فِيْ جَهَنَّمَ خٰلِدُوْنَ ﴿١٠٤﴾ ج

104. Na yule mizani yake itakayokuwa myepesi, basi hao ndio waliojitia hasarani nafsi zao, katika Jahanamu watakaa.

تَلْفَحُ وُجُوْهَهُمُ النَّارُ وَهُمْ فِيْهَا كٰلِحُوْنَ ﴿١٠٥﴾

105. Moto utaziunguza nyuso zao nao humo watafinya nyuso kutokana na maumivu makali.

Aya 97. *Uzuie ubaya kwa yaliyo bora.* Hapa limetolewa fundisho jema kwa namna iliyo bora. Ubaya ni kitu cha kuzuiliwa, lakini uzuiwe kwa njia iliyo bora yo yote iwayo inayoweza kufaa, kama iwe huruma, maombi, nasaha au adhabu.

106. Je, hazikuwa Aya Zangu zikisomwa kwenu lakini mlikuwa mkizikadhibisha?

اَلَمۡ تَكُنۡ اٰيٰتِىۡ تُتۡلٰى عَلَيۡكُمۡ فَكُنۡتُمۡ بِهَا تُكَذِّبُوۡنَ ﴿۱۰۶﴾

107. Watasema: Mola wetu ilitushinda bahati yetu mbaya, na tukawa watu wenye kupotea.

قَالُوۡا رَبَّنَا غَلَبَتۡ عَلَيۡنَا شِقۡوَتُنَا وَكُنَّا قَوۡمًا ضَآلِّيۡنَ ﴿۱۰۷﴾

108. Mola wetu, Tutoe humo, na tufanyapo tena bila shaka tutakuwa wadhalimu.

رَبَّنَاۤ اَخۡرِجۡنَا مِنۡهَا فَاِنۡ عُدۡنَا فَاِنَّا ظٰلِمُوۡنَ ﴿۱۰۸﴾

109. Atasema: Kaeni mbali humo wala msinisemeshe.

قَالَ اخۡسَـُٔوۡا فِيۡهَا وَلَا تُكَلِّمُوۡنِ ﴿۱۰۹﴾

110. Bila shaka palikuwa na kundi katika watumishi Wangu wakisema: Mola wetu, Tumeamini, basi tusamehe na turehemu nawe ndiwe mbora wa wanaorehemu.

اِنَّهٗ كَانَ فَرِيۡقٌ مِّنۡ عِبَادِىۡ يَقُوۡلُوۡنَ رَبَّنَاۤ اٰمَنَّا فَاغۡفِرۡ لَنَا وَارۡحَمۡنَا وَاَنۡتَ خَيۡرُ الرّٰحِمِيۡنَ ﴿۱۱۰﴾

111. Lakini ninyi mliwafanyia mzaha hata wakakusahaulisheni kunikumbuka, na mlikuwa mkiwacheka.

فَاتَّخَذۡتُمُوۡهُمۡ سِخۡرِيًّا حَتّٰۤى اَنۡسَوۡكُمۡ ذِكۡرِىۡ وَكُنۡتُمۡ مِّنۡهُمۡ تَضۡحَكُوۡنَ ﴿۱۱۱﴾

112. Hakika leo Nimewalipa kwa sababu walisubiri, bila shaka hao ndio wenye kufuzu.

اِنِّىۡ جَزَيۡتُهُمُ الۡيَوۡمَ بِمَا صَبَرُوۡۤا ۙ اَنَّهُمۡ هُمُ الۡفَآئِزُوۡنَ ﴿۱۱۲﴾

113. Atasema: Mlikaa muda gani katika ardhi kwa hesabu ya miaka?

قٰلَ كَمۡ لَبِثۡتُمۡ فِى الۡاَرۡضِ عَدَدَ سِنِيۡنَ ﴿۱۱۳﴾

114. Watasema: Tulikaa siku moja au sehemu ya siku, basi waulize wafanyao hesabu.

قَالُوۡا لَبِثۡنَا يَوۡمًا اَوۡ بَعۡضَ يَوۡمٍ فَسۡـَٔـلِ الۡعَآدِّيۡنَ ﴿۱۱۴﴾

Aya 101. Neno *Hapana* linaonyesha ya kuwa mtu akisha kufa harudi tena duniani. Neno *Kalima* maana yake ni *neno* au *tamko.* Pengine hata neno la kafiri limeitwa *kalima.* Kadhalika Nabii Isa kuitwa na Allah *kalima* sio mradi wake ya kuwa yeye ni mungu kama wadhanivyo Wakristo, bali yeye ni matokeo ya neno alilotamka Mungu, "Kuwa," naye akawa.

Neno *Barzakh* tumelifasiri hapa "kinga," na neno hili linaonyesha hali ya katikati ya mtu baada ya kufa na kabla ya kufufuliwa.

Aya 111. *Mlikuwa mkiwacheka.* Katika Aya hii imeelezwa ya kuwa kuwacheka Manabii wa Mungu na watu watawa kunaleta adhabu ya mtu kusahau kumkumbuka Mungu, na moyo wake unakufa.

قٰلَ اِنۡ لَّبِثۡتُمۡ اِلَّا قَلِيۡلًا لَّوۡ اَنَّكُمۡ كُنۡتُمۡ تَعۡلَمُوۡنَ ﴿۱۱۵﴾

115. Atasema: Ninyi hamkukaa ila kidogo - laiti mngalikuwa mmejua!

اَفَحَسِبۡتُمۡ اَنَّمَا خَلَقۡنٰكُمۡ عَبَثًا وَّاَنَّكُمۡ اِلَيۡنَا لَا تُرۡجَعُوۡنَ ﴿۱۱۶﴾

116. Je, mlidhani ya kwamba Tumewaumbeni bure na ya kwamba ninyi Kwetu hamtarudishwa?

فَتَعٰلَى اللّٰهُ الۡمَلِكُ الۡحَقُّ ۚ لَاۤ اِلٰهَ اِلَّا هُوَ ۚ رَبُّ الۡعَرۡشِ الۡكَرِيۡمِ ﴿۱۱۷﴾

117. Basi Ametukuka Allah, Mfalme wa haki; hakuna aabudiwaye ila Yeye, Mola wa Arshi yenye heshima.

وَمَنۡ يَّدۡعُ مَعَ اللّٰهِ اِلٰهًا اٰخَرَ ۙ لَا بُرۡهَانَ لَهٗ بِهٖ ۙ فَاِنَّمَا حِسَابُهٗ عِنۡدَ رَبِّهٖ ؕ اِنَّهٗ لَا يُفۡلِحُ الۡكٰفِرُوۡنَ ﴿۱۱۸﴾

118. Na Anayemwomba pamoja na Allah, mungu mwingine, yeye hana dalili ya (jambo) hili; basi bila shaka hesabu yake iko kwa Mola wake. Kwa hakika makafiri hawafanikiwi.

وَقُلۡ رَّبِّ اغۡفِرۡ وَارۡحَمۡ وَاَنۡتَ خَيۡرُ الرّٰحِمِيۡنَ ﴿۱۱۹﴾ ع

119. Nawe sema: Mola wangu, samehe na rehemu, nawe ndiwe Mbora wa wanaorehemu.

Aya 118. *Makafiri hawafanikiwi.* Matokeo ya makafiri yameelezwa hapa, kama vile mwanzo wa sura yalionyeshwa matokeo ya waaminio, ya kuwa wanaofuata maagizo ya Allah wanafanikiwa, na wanaoyaacha wanaingia katika kufuru na wanashindwa.

Aya 119. Katika Aya hii yamefundishwa maombi ya kujiepusha na kufuru na kujiepusha na matokeo yake mabaya.

سُوْرَةُ النُّوْرِ مَدَنِيَّةٌ وَّ هِيَ مَعَ الْبَسْمَلَةِ خَمْسٌ وَّ سِتُّوْنَ اٰيَةً وَّ تِسْعَةُ رُكُوْعَاتٍ

24. SURA AN-NUUR

Imeteremshwa Madina

Ina mafungu 9 na Aya 65 pamoja na Bismillahi

بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ ①

1. Kwa jina la Allah, Mwingi wa rehema, Mwingi wa ukarimu.

سُوْرَةٌ اَنْزَلْنٰهَا وَ فَرَضْنٰهَا وَاَنْزَلْنَا فِيْهَآ اٰيٰتٍۭ بَيِّنٰتٍ لَّعَلَّكُمْ تَذَكَّرُوْنَ ②

2. Ni sura Tumeiteremsha, na Tumeilazimisha, na Tumeteremsha ndani yake Aya zilizo wazi ili mpate kushika nasaha.

اَلزَّانِيَةُ وَالزَّانِيْ فَاجْلِدُوْا كُلَّ وَاحِدٍ مِّنْهُمَا مِائَةَ جَلْدَةٍ ۖ وَّلَا تَاْخُذْكُمْ بِهِمَا رَاْفَةٌ فِيْ دِيْنِ اللّٰهِ اِنْ كُنْتُمْ تُؤْمِنُوْنَ بِاللّٰهِ وَالْيَوْمِ الْاٰخِرِ ۚ وَ لْيَشْهَدْ عَذَابَهُمَا طَآئِفَةٌ مِّنَ الْمُؤْمِنِيْنَ ③

3. Mzinifu mwanamke na mzinifu mwanamume, basi mpigeni kila mmoja wao mijeledi mia. Wala isiwashikeni kwa ajili yao huruma katika hukumu ya Allah, ikiwa ninyi mnamwamini Allah na siku ya Mwisho; na lishuhudie adhabu yao kundi la waaminio.

اَلزَّانِيْ لَا يَنْكِحُ اِلَّا زَانِيَةً اَوْ مُشْرِكَةً ۫ وَّ الزَّانِيَةُ لَا يَنْكِحُهَآ اِلَّا زَانٍ اَوْ مُشْرِكٌ ۚ وَحُرِّمَ ذٰلِكَ عَلَى الْمُؤْمِنِيْنَ ④

4. Mwanamume mzinifu hafungamani ila na mwanamke mzinifu au mwanamke mshirikina; na mwanamke mzinifu hafungamani naye ila mwanamume mzinifu au mshirikina; na hayo yameharamishwa kwa waaminio.

Jina la sura hii *Nuru* limetoka katika Aya 36 ambayo inaeleza kuwa Islam ndiyo nuru iliyokamilika ya Allah inayong'aa mashariki na magharibi.

Sura hii nzima ilishuka Madina. Sehemu zingine za sura hii zinaweza kujulikana tarehe ziliposhuka. Kama sehemu ile inayoeleza kusingiziwa kwa Bibi Aisha ambayo ilishuka mwezi mmoja baada ya kurudi kutoka vita ya Bani Mustalik katika mwezi wa Sha'baan mwaka wa tano wa Hijra.

Aya 2. *Ni sura Tumeiteremsha, na Tumeilazimisha.* Sio mradi wa maneno haya kwamba sura zingine hazikuteremshwa na kufaridhishwa, la. Bali hapa Allah anatoa habari ya kuwa mambo yaliyomo katika sura hii ni muhimu kabisa katika makao mema na maendeleo yenye raha, kwa hiyo yanatakiwa kusikilizwa sawasawa, na habari zote zifuatwe kabisa.

Aya 3. *Wala isiwashikeni kwa ajili yao huruma.* Ziko namna za adhabu ambazo humletea

وَالَّذِيْنَ يَرْمُوْنَ الْمُحْصَنٰتِ ثُمَّ لَمْ يَاْتُوْا
بِاَرْبَعَةِ شُهَدَآءَ فَاجْلِدُوْهُمْ ثَمٰنِيْنَ
جَلْدَةً وَّلَا تَقْبَلُوْا لَهُمْ شَهَادَةً اَبَدًا ۚ
وَاُولٰٓئِكَ هُمُ الْفٰسِقُوْنَ ۙ﴿۴﴾

5. Na wale wanaowasingizia wanawake waaminifu kisha hawaleti mashahidi wanne, basi wapigeni mijeledi themanini na msiwakubalie ushahidi wao kamwe, na hao ndio mafasiki;

اِلَّا الَّذِيْنَ تَابُوْا مِنْۢ بَعْدِ ذٰلِكَ وَاَصْلَحُوْا ۚ
فَاِنَّ اللّٰهَ غَفُوْرٌ رَّحِيْمٌ ﴿۵﴾

6. Isipokuwa wale waliotubu na kujirekebisha baada ya hayo, basi bila shaka Allah ni Msamehevu, Mrehemevu.

وَالَّذِيْنَ يَرْمُوْنَ اَزْوَاجَهُمْ وَلَمْ يَكُنْ
لَّهُمْ شُهَدَآءُ اِلَّآ اَنْفُسُهُمْ فَشَهَادَةُ
اَحَدِهِمْ اَرْبَعُ شَهٰدٰتٍۭ بِاللّٰهِ ۙ اِنَّهٗ
لَمِنَ الصّٰدِقِيْنَ ﴿۶﴾

7. Na wale wanaowasingizia wake zao na hawana mashahidi ila nafsi zao, basi ushahidi wa mmoja wao utakuwa kushahidilia mara nne kwa kiapo cha Allah: ya kwamba bila shaka yeye ni miongoni mwa wakweli.

وَالْخَامِسَةُ اَنَّ لَعْنَتَ اللّٰهِ عَلَيْهِ اِنْ كَانَ
مِنَ الْكٰذِبِيْنَ ﴿۷﴾

8. Na mara ya tano (aape) kwamba laana ya Allah iwe juu yake ikiwa yu miongoni mwa waongo.

وَيَدْرَؤُا عَنْهَا الْعَذَابَ اَنْ تَشْهَدَ اَرْبَعَ
شَهٰدٰتٍۭ بِاللّٰهِ ۙ اِنَّهٗ لَمِنَ الْكٰذِبِيْنَ ۙ﴿۸﴾

9. Na (mkewe) itamwondolea adhabu kwa kutoa ushuhuda mara nne kwa kiapo cha Allah ya kwamba huyu (mume) ni miongoni mwa waongo.

وَالْخَامِسَةَ اَنَّ غَضَبَ اللّٰهِ عَلَيْهَآ اِنْ كَانَ
مِنَ الصّٰدِقِيْنَ ﴿۹﴾

10. Na mara ya tano (aape) ya kwamba hasira ya Allah iwe juu yake kama (mumewe) yu miongoni mwa wakweli.

---

mtu taabu na watu wakamhurumia. Mathalan mtu ameanguka ghafla na watu wanamhurumia. Lakini mtu akivunja Sheria ya Allah, basi sasa hakuna huruma anayostahili kuonyeshwa ili kuondoa adhabu iliyowekwa na Allah. Kama mtu anafanya zinaa au aibe atalazimika kuadhibiwa, na hakuna mtu mwenye haki ya kuzuia adhabu yake.

Aya 5. Aya hii imeweka adhabu namna tatu kwa watu wanaowalaumu wanawake kwa mambo ya zinaa, kisha wasiweze kuleta mashahidi wasiopungua wanne walio wema. Adhabu ya kwanza ni ya mwili: apigwe mijeledi themanini: adhabu ya pili ni ya heshima yake: asikubaliwe kutoa ushahidi juu ya jambo lo lote; adhabu ya tatu ni juu ya roho yake kwamba anakuwa mtu mbaya.

Aya 7-10. Aya hizi zimeeleza habari za mume na mke wanaosingiziana, kuwa waapizane, na namna ya kuapizana huko imeelezwa ndani ya Aya hii hii. Kadhalika Sheria ya Kiislamu

وَلَوْلَا فَضْلُ اللّٰهِ عَلَيْكُمْ وَرَحْمَتُهٗ وَاَنَّ
اللّٰهَ تَوَّابٌ حَكِيْمٌ ﴿١١﴾ ع

11. Na (mngetaabika) lau isingalikuwa fadhili ya Allah juu yenu na rehema Yake, na ya kuwa Allah ni Mpokeaji wa toba, Mwenye hekima

FUNGU 2

اِنَّ الَّذِيْنَ جَآءُوْ بِالْاِفْكِ عُصْبَةٌ
مِّنْكُمْ ؕ لَا تَحْسَبُوْهُ شَرًّا لَّكُمْ ؕ بَلْ هُوَ
خَيْرٌ لَّكُمْ ؕ لِكُلِّ امْرِئٍ مِّنْهُمْ مَّا
اكْتَسَبَ مِنَ الْاِثْمِ ۚ وَالَّذِيْ تَوَلّٰى
كِبْرَهٗ مِنْهُمْ لَهٗ عَذَابٌ عَظِيْمٌ ﴿١٢﴾

12. Hakika wale walioleta uwongo ni kundi miongoni mwenu. Msiufikiri u shari kwenu, bali huo ni heri kwenu. Kila mtu kati yao atapata aliyoyachuma katika dhambi. Na yule aliyeitawala sehemu yake kubwa miongoni mwao, atapata adhabu kubwa.

لَوْلَآ اِذْ سَمِعْتُمُوْهُ ظَنَّ الْمُؤْمِنُوْنَ
وَالْمُؤْمِنٰتُ بِاَنْفُسِهِمْ خَيْرًا ۙ وَّقَالُوْا هٰذَآ
اِفْكٌ مُّبِيْنٌ ﴿١٣﴾

13. Mbona mlipousikia; wanaume waaminio na wanawake waaminio hawakuwadhania wenzao mema, na kusema: Huu ni uzushi dhahiri?

لَوْلَا جَآءُوْ عَلَيْهِ بِاَرْبَعَةِ شُهَدَآءَ ۚ
فَاِذْ لَمْ يَاْتُوْا بِالشُّهَدَآءِ فَاُولٰٓئِكَ عِنْدَ اللّٰهِ
هُمُ الْكٰذِبُوْنَ ﴿١٤﴾

14. Mbona hawakuleta mashahidi wanne? Na walipokosa kuleta mashahidi, basi hao mbele ya Allah ndio waongo.

وَلَوْلَا فَضْلُ اللّٰهِ عَلَيْكُمْ وَرَحْمَتُهٗ فِي
الدُّنْيَا وَالْاٰخِرَةِ لَمَسَّكُمْ فِيْ مَآ اَفَضْتُمْ
فِيْهِ عَذَابٌ عَظِيْمٌ ﴿١٥﴾ ع

15. Na kama isingalikuwa juu yenu fadhili ya Allah na rehema Yake katika dunia na Akhera, bila shaka ingaliwaguseni, kwa sababu ya yale mliyoyashughulikia, adhabu kubwa.

اِذْ تَلَقَّوْنَهٗ بِاَلْسِنَتِكُمْ وَتَقُوْلُوْنَ
بِاَفْوَاهِكُمْ مَّا لَيْسَ لَكُمْ بِهٖ عِلْمٌ
وَّتَحْسَبُوْنَهٗ هَيِّنًا ۖ وَّهُوَ عِنْدَ اللّٰهِ عَظِيْمٌ ﴿١٦﴾

16. Mlipoupokea kwa ndimi zenu na mkasema kwa vinywa vyenu msiyoyajua, na mliufikiri ni jambo dogo, kumbe mbele ya Allah ni kubwa.

---

imeeleza ya kwamba kuapizana huko kufanywe mbele za watu na mahali patakatifu. Anayeapa anapokaribia kuomba laana ya Allah afahamishwe kuwa kama atasema uwongo laana ya Mungu itamshukia na atakuwa katika balaa kubwa.

Aya 12. Walioleta uzushi huu ni wanafiki. Safari moja Mtume *s.a.w.* alikuwa akirudi katika mapigano na Banu Mustali. Mkewe Bibi Aisha alikuwa pamoja naye. Kulipokuwa bado giza Bibi Aisha alikuwa akitafuta kidani chake alichokuwa amekiazima, na walinzi wake wakafunga

17. Na mbona, mlipousikia, hamkusema: Haitupasi tuzungumze haya: Utakatifu ni Wako, haya ni masingizio makubwa.

وَلَوْلَآ اِذْ سَمِعْتُمُوْهُ قُلْتُمْ مَّا يَكُوْنُ لَنَآ اَنْ نَّتَكَلَّمَ بِهٰذَا ۖ سُبْحٰنَكَ هٰذَا بُهْتَانٌ عَظِيْمٌ ﴿١٧﴾

18. Allah Anawanasihini ya kwamba msirudie kabisa mfano wa haya, ikiwa ninyi ni waaminio.

يَعِظُكُمُ اللّٰهُ اَنْ تَعُوْدُوْا لِمِثْلِهٖٓ اَبَدًا اِنْ كُنْتُمْ مُّؤْمِنِيْنَ ﴿١٨﴾

19. Na Allah Anawabainishieni Ishara; na Allah ndiye Ajuaye, Mwenye hekima.

وَيُبَيِّنُ اللّٰهُ لَكُمُ الْاٰيٰتِ ۭ وَاللّٰهُ عَلِيْمٌ حَكِيْمٌ ﴿١٩﴾

20. Kwa yakini wale wanaopenda uenee ouvu katika wale walioamini, watapata adhabu iumizayo katika dunia na Akhera; na Allah Anajua na ninyi hamjui.

اِنَّ الَّذِيْنَ يُحِبُّوْنَ اَنْ تَشِيْعَ الْفَاحِشَةُ فِي الَّذِيْنَ اٰمَنُوْا لَهُمْ عَذَابٌ اَلِيْمٌ ۙ فِي الدُّنْيَا وَالْاٰخِرَةِ ۭ وَاللّٰهُ يَعْلَمُ وَاَنْتُمْ لَا تَعْلَمُوْنَ ﴿٢٠﴾

21. Na (yangetokea machafuko makubwa) isingalikuwa fadhili ya Allah juu yenu na rehema Yake, na ya kuwa Allah ni Mpole, Mwenye huruma.

وَلَوْلَا فَضْلُ اللّٰهِ عَلَيْكُمْ وَرَحْمَتُهٗ وَاَنَّ اللّٰهَ رَءُوْفٌ رَّحِيْمٌ ﴿٢١﴾ ع ٢

FUNGU 3

22. Enyi mlioamini! msifuate nyayo za Shetani; na atakayefuata nyayo za Shetani, basi hakika yeye huamrisha mambo ya aibu na maovu; na lau isingekuwa

يٰٓاَيُّهَا الَّذِيْنَ اٰمَنُوْا لَا تَتَّبِعُوْا خُطُوٰتِ الشَّيْطٰنِ ۭ وَمَنْ يَّتَّبِعْ خُطُوٰتِ الشَّيْطٰنِ فَاِنَّهٗ يَاْمُرُ بِالْفَحْشَاۗءِ وَالْمُنْكَرِ ۭ وَلَوْلَا

---

safari wakidhania yumo ndani ya banda lake juu ya ngamia. Bibi Aisha aliporudi akakuta watu wote wameshaondoka, basi akakaa pale pale na kuanza kutaabika hata akapitiwa na usingizi. Huku nyuma alikuwa akija Bwana Safwan ambaye alikuwa amewekwa nyuma kabisa, kama ilivyokuwa desturi ya Mtume, huenda akaweza kuokota cho chote kilichosahauliwa na watu katika kambi. Safwan alimkuta Bibi Aisha pale na akashtuka. Akashuka juu ya ngamia wake na Bibi Aisha akakaa juu yake, na Safwana akaja naye akitembea mpaka Madina. Wanafiki kuona hivi wakaanza kueneza habari za uwongo wakimsingizia Bibi Aisha na Safwan. Ndipo Allah akateremsha Aya hizi kuhakikisha usafi wa Bibi Aisha na uwongo wa wanafiki.

Aliyetawala sehemu yake kubwa ni Abdullah bin Ubayy bin Salul mkubwa wa wanafiki (Bukhari).

Aya 18. *Ikiwa ninyi ni waaminio.* Ndio kusema kujiingiza katika masingizio ya namna hii ni jambo ovu kabisa na linamtoa mtu katika imani; na hapa Allah anawaonya waaminio wasirejee kamwe katika uovu wa namna hii. Ni masikitiko namna gani kuona jinsi Waislamu wanavyopuuza mafundisho haya mema.

فَضْلُ اللّٰهِ عَلَيْكُمْ وَ رَحْمَتُهٗ مَا زَكٰى
مِنْكُمْ مِّنْ اَحَدٍ اَبَدًا ۙ وَّ لٰكِنَّ اللّٰهَ يُزَكِّيْ
مَنْ يَّشَآءُ ؕ وَاللّٰهُ سَمِيْعٌ عَلِيْمٌ ﴿٢٢﴾

fadhili za Allah na rehema Zake asingalitakasika kamwe miongoni mwenu hata mmoja ; lakini Allah Humtakasa Amtakaye, na Allah ni Asikiaye, Ajuaye.

وَلَا يَاْتَلِ اُولُوا الْفَضْلِ مِنْكُمْ وَالسَّعَةِ
اَنْ يُّؤْتُوْٓا اُولِي الْقُرْبٰى وَالْمَسٰكِيْنَ
وَالْمُهٰجِرِيْنَ فِيْ سَبِيْلِ اللّٰهِ ۖ وَلْيَعْفُوْا
وَلْيَصْفَحُوْا ؕ اَلَا تُحِبُّوْنَ اَنْ يَّغْفِرَ اللّٰهُ
لَكُمْ ؕ وَاللّٰهُ غَفُوْرٌ رَّحِيْمٌ ﴿٢٣﴾

23. Na wasiape wale wenye utajiri na wenye wasaa (kujizuia) kuwapa walio jamaa, na maskini na waliohama katika njia ya Allah, na wasamehe na waachilie. Je, ninyi hampendi Allah Awasameheni? Na Allah ni Msamehevu, Mrehemevu.

اِنَّ الَّذِيْنَ يَرْمُوْنَ الْمُحْصَنٰتِ الْغٰفِلٰتِ
الْمُؤْمِنٰتِ لُعِنُوْا فِي الدُّنْيَا وَالْاٰخِرَةِ ۪
وَلَهُمْ عَذَابٌ عَظِيْمٌ ﴿٢٤﴾

24. Bila shaka wale wanaowasingizia wanawake waliotakasika, wasiokumbuka (maovu), waaminio, wamelaaniwa katika dunia na Akhera, nao watapata adhabu kubwa.

يَّوْمَ تَشْهَدُ عَلَيْهِمْ اَلْسِنَتُهُمْ وَاَيْدِيْهِمْ
وَاَرْجُلُهُمْ بِمَا كَانُوْا يَعْمَلُوْنَ ﴿٢٥﴾

25. Siku ambayo zitawashuhudia ndimi zao, na mikono yao, na miguu yao, kwa yale waliyokuwa wakiyafanya.

يَوْمَئِذٍ يُّوَفِّيْهِمُ اللّٰهُ دِيْنَهُمُ الْحَقَّ
وَيَعْلَمُوْنَ اَنَّ اللّٰهَ هُوَ الْحَقُّ الْمُبِيْنُ ﴿٢٦﴾

26. Siku hiyo Allah Atawapa sawasawa malipo yao ya haki, na watajua kwamba Allah ndiye haki dhahiri.

اَلْخَبِيْثٰتُ لِلْخَبِيْثِيْنَ وَالْخَبِيْثُوْنَ
لِلْخَبِيْثٰتِ ۚ وَالطَّيِّبٰتُ لِلطَّيِّبِيْنَ
وَالطَّيِّبُوْنَ لِلطَّيِّبٰتِ ۚ اُولٰٓئِكَ
مُبَرَّءُوْنَ مِمَّا يَقُوْلُوْنَ ؕ لَهُمْ
مَّغْفِرَةٌ وَّ رِزْقٌ كَرِيْمٌ ﴿٢٧﴾ ع ٣ ٩

27. Wanawake wabaya ni kwa ajili ya wanaume wabaya, na wanaume wabaya ni kwa ajili ya wanawake wabaya; na wanawake wema ni kwa ajili ya wanaume wema, na wanaume wema ni kwa ajili ya wanawake wema; hao wameepushwa na hayo wanayoyasema, wao watapata msamaha na riziki yenye heshima.

Aya 23. Aya hii inaeleza habari za Seyidna Abu Bakar ambaye aliapa kuwa hatampa matumizi jamaa yake mmoja aitwaye Mistah kwa kuwa alijiingiza katika kueneza habari za uwongo juu ya Aisha. Allah katika Aya hii anakataza kiapo hicho na anafundisha ya kuwa mwenye nafasi asiache kumpa matumizi jamaa yake.

FUNGU 4

28. Enyi mlioamini! Msiingie nyumba ambazo si nyumba zenu mpaka mwombe ruhusa, na mwatolee salamu waliomo humo. Hayo ni bora kwenu, ili mpate kushika nasaha.

يٰٓاَيُّهَا الَّذِيْنَ اٰمَنُوْا لَا تَدْخُلُوْا بُيُوْتًا
غَيْرَ بُيُوْتِكُمْ حَتّٰى تَسْتَاْنِسُوْا وَتُسَلِّمُوْا
عَلٰٓى اَهْلِهَا ؕ ذٰلِكُمْ خَيْرٌ لَّكُمْ
لَعَلَّكُمْ تَذَكَّرُوْنَ ﴿٢٨﴾

29. Na kama hamtamkuta humo ye yote, basi msiingie mpaka mmeruhu-siwa. Na mkiambiwa, Rudini; basi rudini; hili ni takaso kwenu. Na Allah Anayajua mnayoyatenda.

فَاِنْ لَّمْ تَجِدُوْا فِيْهَآ اَحَدًا فَلَا تَدْخُلُوْهَا
حَتّٰى يُؤْذَنَ لَكُمْ ۚ وَاِنْ قِيْلَ لَكُمُ
ارْجِعُوْا فَارْجِعُوْا هُوَ اَزْكٰى لَكُمْ ؕ وَاللّٰهُ
بِمَا تَعْمَلُوْنَ عَلِيْمٌ ﴿٢٩﴾

30. Si vibaya kwenu kuingia ma-jumba yasiyokaliwa mlimo na manufaa yenu; na Allah Anayajua mnayoyadhi-hirisha na mnayoyaficha.

لَيْسَ عَلَيْكُمْ جُنَاحٌ اَنْ تَدْخُلُوْا بُيُوْتًا
غَيْرَ مَسْكُوْنَةٍ فِيْهَا مَتَاعٌ لَّكُمْ ؕ وَاللّٰهُ
يَعْلَمُ مَا تُبْدُوْنَ وَمَا تَكْتُمُوْنَ ﴿٣٠﴾

31. Waambie waaminio wanaume wainamishe macho yao, na wazilinde tupu zao, hili ni takaso kwao; Bila shaka Allah Anazo habari za yale wanayoya-fanya.

قُلْ لِّلْمُؤْمِنِيْنَ يَغُضُّوْا مِنْ اَبْصَارِهِمْ
وَيَحْفَظُوْا فُرُوْجَهُمْ ؕ ذٰلِكَ اَزْكٰى لَهُمْ ؕ
اِنَّ اللّٰهَ خَبِيْرٌۢ بِمَا يَصْنَعُوْنَ ﴿٣١﴾

32. Na waambie wanawake waami-nio kwamba wainamishe macho yao na wazilinde tupu zao, na wasidhihirishe uzuri wao isipokuwa ule uliyo bayana katika hayo, na kwamba washushe shungi zao mpaka vifuani mwao, na wasionyeshe uzuri wao isipokuwa kwa waume zao, au kwa baba zao au kwa baba za waume zao, au kaka

وَقُلْ لِّلْمُؤْمِنٰتِ يَغْضُضْنَ مِنْ اَبْصَارِهِنَّ
وَيَحْفَظْنَ فُرُوْجَهُنَّ وَلَا يُبْدِيْنَ
زِيْنَتَهُنَّ اِلَّا مَا ظَهَرَ مِنْهَا وَلْيَضْرِبْنَ
بِخُمُرِهِنَّ عَلٰى جُيُوْبِهِنَّ ۖ وَلَا يُبْدِيْنَ
زِيْنَتَهُنَّ اِلَّا لِبُعُوْلَتِهِنَّ اَوْ اٰبَآئِهِنَّ
اَوْ اٰبَآءِ بُعُوْلَتِهِنَّ اَوْ اَبْنَآئِهِنَّ اَوْ اَبْنَآءِ

Aya 29. *Mkiambiwa, Rudini, basi rudini.* Kama mtu hakukaribishwa katika nyumba na ameambiwa arudi basi asichukie, bali arudi tu.

Aya 31-32. Aya hizi zinaeleza mafundisho yanayoweza kumpa mtu utawa. Injili inafundisha kuwa mtu asitazame kwa nia mbaya; lakini hii ni upuuzi maana nia mbaya huja

zao au wana wa kaka zao au wana wa dada zao au wanawake wenzao au wale waliomilikiwa na mikono yao ya kuume au wale miongoni mwa watumishi wa nyumbani wa kiume ambao hawana uovu nafsini mwao, au watoto wadogo ambao hawajafikia umri wa kuwa na wazo lo lote kuhusu sehemu za siri za wanawake. Na wasitembee kwa namna ambayo inafichua uzuri waliouficha. Na tubieni nyote kwa Allah enyi waaminio, ili mpate kufaulu.

بُعُوْلَتِهِنَّ اَوْ اِخْوَانِهِنَّ اَوْ بَنِيْٓ اِخْوَانِهِنَّ
اَوْ بَنِيْٓ اَخَوٰتِهِنَّ اَوْ نِسَآئِهِنَّ اَوْ مَا مَلَكَتْ
اَيْمَانُهُنَّ اَوِ التّٰبِعِيْنَ غَيْرِ اُولِي الْاِرْبَةِ
مِنَ الرِّجَالِ اَوِ الطِّفْلِ الَّذِيْنَ لَمْ
يَظْهَرُوْا عَلٰى عَوْرٰتِ النِّسَآءِ ۪ وَلَا
يَضْرِبْنَ بِاَرْجُلِهِنَّ لِيُعْلَمَ مَا يُخْفِيْنَ
مِنْ زِيْنَتِهِنَّ ؕ وَتُوْبُوْٓا اِلَى اللّٰهِ جَمِيْعًا
اَيُّهَ الْمُؤْمِنُوْنَ لَعَلَّكُمْ تُفْلِحُوْنَ ۝٣١

baada ya kuona na kutazama. Qur'an tu ndiyo iliyofunga milango yote ya kupenyea uchafu moyoni.

Mapambo. Neno ambalo tumelifasiri "mapambo" katika Aya hii ni *zinaat* ambalo kwa Kiarabu lina maana hizi: mapambo, na kila sehemu inayoshawishi na kuvuta ya mwanamke, kama umbo lake na uso, na uzuri wa mwili n.k.w.

Isipokuwa yale yaliyodhihirika, yaani yaliyolazimika, yasiyo katika uwezo wa mwanamke, kama mathalan hana nguo, au kwa sababu ya ugonjwa, au kwa sababu ya kazi na mengineyo.

Waangushe shungi zao, yaani shungi zitoke kisogoni zipite juu ya kichwa, zifunike uso, zishuke mpaka vifuani. Lakini wanaweza kuonyesha mapambo yao kwa jamaa zao ambao ni hao tu waliotajwa katika Aya hii.

Wanawake wao. Wanawake wengine wasio jamaa zao wamekatazwa kuchanganyika ovyo nao. Maana wanawake mara nyingi wamekuwa sababu ya fitina. Hufika majumbani na kupeleka nje habari za wanawake wanaowaona na wanakuwa waletao vishawishi na fitina kubwa. Hivyo Aya hii imewakatalia wanawake ovyo pia kuingia majumbani mwa watu, na kadhalika wanawake waaminio wamekatazwa kuonyesha mapambo na uzuri wao kwa wanawake ovyo.

Wala wasipige miguu yao. Inaonyesha ya kuwa ngoma na dansi na michezo ya namna hii imekatazwa.

Dini ya Kiislamu, kama ambavyo mmeona, hairuhusu kabisa kuchanganyika wanaume na wanawake wasio ndugu walioharimishwa kuoana, wacha mbali kugusana. Dansi na michezo iliyo kama hiyo ni mambo yanayotoa nafasi kubwa ya kuchanganyika ovyo wanawake na wanaume kwa namna ambayo imeharimishwa na Allah na Mtume Wake *s.a.w.* Wale wanaofikiri ya kwamba dansi ni katika mambo ya ustaarabu wanakosa kabisa, maana maovu mengi yanatokana na jambo hili kwa kadiri ambayo tabia za watu, hasa vijana, zinaharibika kabisa, na kuwafanya wasiwe na madaraka juu ya nafsi zao.

Waafrika wenye busara wamekwisha ona hatari ya dansi. Kwa mfano, Waziri Mkuu (Katikiro) wa Buganda, Bwana Paulo Kavuma, anasadiki ya kwamba "tokeapo uharibifu mwingi umetokea kati ya vijana wa nchi kwa ajili ya uhusiano unaotokana na dansi na ya kwamba serikali ya Buganda imo katika kufikiria kukomesha kabisa dansi ya Kizungu" (*East African* Standard, Monday, January 19, 1953).

Kwa hakika ngoma na dansi yamefanana na sumu iliyopakaliwa sukari, ambayo utamu wa sukari unamvuta mlaji kuila sumu na kumwua. Watu wenye busara hujiepusha na furaha hizi zisizo na maana. Ustaarabu wa kweli ni ule ambao Allah ameufundisha katika Qur'an toka miaka karibu 1,400 iliyopita, na ambao wenye fikira katika wakuu wa dunia wameanza kufikiri na kuona uzuri au hatari za mambo kama vile yalivyoelezwa na Allah Mjuzi, Mwenye hekima, katika Kitabu Chake hiki cha Qur'an.

وَاَنْكِحُوا الْاَيَامٰى مِنْكُمْ وَالصّٰلِحِيْنَ مِنْ
عِبَادِكُمْ وَاِمَآئِكُمْ ؕ اِنْ يَّكُوْنُوْا
فُقَرَآءَ يُغْنِهِمُ اللّٰهُ مِنْ فَضْلِهٖ ؕ وَاللّٰهُ
وَاسِعٌ عَلِيْمٌ ﴿٣٣﴾

33. Na waozeni wajane miongoni mwenu, na walio wema katika watumwa wenu, na wajakazi wenu; kama watakuwa mafukara, Allah Atawatajirisha kwa fadhili Zake; na Allah ni Mwenye wasaa, Mwenye kujua.

وَلْيَسْتَعْفِفِ الَّذِيْنَ لَا يَجِدُوْنَ نِكَاحًا
حَتّٰى يُغْنِيَهُمُ اللّٰهُ مِنْ فَضْلِهٖ ؕ وَالَّذِيْنَ
يَبْتَغُوْنَ الْكِتٰبَ مِمَّا مَلَكَتْ اَيْمَانُكُمْ
فَكَاتِبُوْهُمْ اِنْ عَلِمْتُمْ فِيْهِمْ خَيْرًا ۖ
وَّاٰتُوْهُمْ مِّنْ مَّالِ اللّٰهِ الَّذِيْٓ اٰتٰىكُمْ ؕ
وَلَا تُكْرِهُوْا فَتَيٰتِكُمْ عَلَى الْبِغَآءِ
اِنْ اَرَدْنَ تَحَصُّنًا لِّتَبْتَغُوْا عَرَضَ
الْحَيٰوةِ الدُّنْيَا ؕ وَمَنْ يُّكْرِهْهُّنَّ فَاِنَّ
اللّٰهَ مِنْۢ بَعْدِ اِكْرَاهِهِنَّ غَفُوْرٌ رَّحِيْمٌ ﴿٣٤﴾

34. Na washike utawa wale wasiopata kuoa mpaka Allah Awatajirishe kwa fadhili Zake. Na wale wanaotaka hati katika wale inayowamiliki mikono yenu ya kuume, basi waandikieni, kama mkiona wema kwao. Na wapeni katika mali ya Allah Aliyowapeni. Wala msiwashurutishe vijana wenu wa kike kufanya ukahaba kama wakitaka kukaa utawani, ili kutafuta vifaa vya maisha ya dunia. Na Atakayewashurutisha, basi hakika Allah baada ya kushurutishwa kwao ni Msamehevu, Mrehemevu.

Aya 34. *Na wale wanaotaka hati.* Utumwa umeenea duniani zamani sana kabla ya kufika Uislamu. Katika vitabu vya Wakristo vya Maagano ya Kale zinafundishwa kanuni za kufuga watumwa na kuwanunua. Mathalan, wanaambiwa, "Ukinunua mtumwa Mwebrania, miaka sita atatumika: wa saba atatoka huru . . . lakini mtumwa akinena nampenda bwana wangu . . . . basi bwana atamleta kwa Mungu, atamleta kwa mlangoni au karibu na ngazi ya mlango: na bwana wake atamtoboa sikio kwa uma; atamtumikia milele" (Kutoka 21:2-6). Tena wameambiwa, "Mtu akimpiga mtumwa wake, au mjakazi wake, kwa fimbo, naye akafa mkononi mwake, atalipa kisasi. Lakini akipata kusimama siku moja mbili, hapana kisasi: kwani mali yake yeye" (Kutoka 21:20).

Katika siku za Yesu Kristo kulikuwa na watumwa. Yeye hakusema neno lo lote juu ya watumwa waliokuwako. Bali tunaona wafuasi wake, kama Paulo, badala ya kutoa maagizo ya kuwafungulia watumwa, na kukataza watu kufuga watumwa, anatoa maagizo kama haya kuwaambia watumwa, na anasema, "Ninyi watumwa, watiini hao ambao kwa mwili ni bwana zenu, katika mambo yote" (Wakolosai 3:22); "Enyi watumwa, watiini walio bwana zenu kwa jinsi ya mwili, kwa hofu na kutetemeka, kwa unyofu wa moyo, kana kwamba ni kumtii Kristo" (Waefaso, 6:5).

Alipofika Mtume Muhammad *s.a.w.* alikuta duniani utumwa unawapa watu dhiki nyingi. Basi Uislamu mara ulishika kazi ya kuondoa watumwa. Jambo la kwanza alilofanya Mtume *s.a.w.* ni kuona hesabu ya watumwa isiongezeke kwa kutiwa utumwani watu walio huru. Mtume

s.a.w. akasema, "Allah ameniambia kuwa kuna watu watatu ambao atahasimiana nao siku ya Kiyama: (1) Mtu anayeahidiana kwa jina Lake, kisha akavunja ahadi, (2) mtu anayemwuza mtu huru na kula thamani yake na (3) mtu anayempagaza mpagazi, kisha hampi ujira wake" (Bukhari). Tena akasema, "Anayemchukua mtu huru na kumtia utumwani, Sala zake hazipokelewi" (Abu Daudi).

Baada ya kuufunga mlango wa kuingizia watumwa wapya, fundisho jingine la Uislamu lilikuwa kuwafungulia watumwa waliokuwapo, na kuwapa uhuru. Uislamu ukatilia mkazo kabisa juu ya kuwaweka huru watumwa. Katika nyakati za mwanzo wa kazi yake, Mtume aliteremshiwa ufunuo juu ya kuwaweka huru watumwa. Allah anasema, *"Je! Hatukumpa (mtu) macho mawili, na ulimi, na midomo miwili, na Tukamwonyesha njia mbili zilizoinuka? Lakini hakupita njia ya mlimani. Na nini kitakujulisha njia ya mlimani ni nini? Ni kumpa mtumwa uungwana, au kumlisha siku ya njaa, yatima jamaa au maskini hohe hahe"* (sura 90:9-17).

Mtume *s.a.w.* alisema "Mtu ye yote amwekaye huru mtumwa Mwislamu, Mungu atamwokoa na moto wa Jahanamu, kiungo kwa kiungo" (Bukhari). Mwarabu mmoja alimwendea Mtume *s.a.w.* akauliza, "Ee Nabii wa Mungu, nijulishe kazi ya kufanya ambayo itanipeleka moja kwa moja Peponi." Mtume akajibu: "Swali lako ni fupi, lakini umeuliza jambo kubwa. Weka huru mtumwa; na kama huwezi kufanya hivyo peke yako, fanya kwa ushirika na wengine" (Baihaki). Baba wa Abu Burdah anasimulia ya kuwa, Mtume alikuwa akisema, "Kama mmoja wenu ana mjakazi na anampa elimu nzuri na mafunzo bora, na mwisho anamweka huru na kumwoa, atakuwa na thawabu mara mbili" (Bukhari).

Islam hata imeamuru kuweka huru mtumwa kama fidia ya baadhi ya makosa. Soma, sura 4:93; sura 5:90; sura 58:4. Ukisoma Aya hizi utaona ya kuwa kuweka huru mtumwa ndilo jambo la kwanza, na mtu akosapo mtumwa ndipo afanye sharti zingine. Hii inaonyesha wazi kuwa shabaha ya Uislamu ilikuwa ni kuondoa kabisa utumwa.

"Mtume aliamuru kuweka huru watumwa linapopatwa jua" (Bukhari). Mtu mmoja alimpiga kofi moja mtumwa aliyekuwa wa shirika baina yake yeye na nduguze. Mtu huyo anasema, "Mtume s.a.w. akapata kujua habari hii, naye akatuamuru kumweka huru mtumwa yule" (Muslim). Na ibni Omar, ambaye amesimulia habari hii, ameongezea kusema ya kuwa mtu anayemweka huru mtumwa kwa sababu amempiga hastahili thawabu yo yote, maana Islam huamuru kuweka huru mtumwa kuwa ndiyo fidia ya kumpiga, na adhabu iliyoamriwa haiwezi kuwa na thawabu (Muslim). Linganisha agizo hili na lile la Biblia katika chuo cha Kutoka 21:20 nawe utaona kuna hitilafu kubwa kati ya ubaya wa mafundisho yao na uzuri wa mafundisho ya Uislamu.

Mtume *s.a.w.* alisema, "Kama mtu ye yote akiwa na mtumwa aliye jamaa yake, ampe uhuru mara moja" Ibni Maja).

Mtu akiwa na Mtumwa wa shirika na wenziwe, yeye akimwacha huru upande wake, hutakiwa alipe kwa washirika wenziwe ili mtumwa huyo awe huru kabisa. Lakini kama hana mali, hata hivyo mtumwa huyo atakuwa huru kabisa ili afanye kazi ya kuwalipa mabwana zake wengine, na atapewa kila namna ya msaada. (Bukhari).

Watumwa wa makafiri walikimbilia kwa Mtume s.a.w., Madina, wakitoka Makka. Mabwana zao waliombwa warudishiwe watumwa wao, na baadhi ya Waislamu wakakubali, lakini Mtume alikasirika sana akakataa kuwarudisha, akisema, "Ni watu huru wa Mungu, je niwarudishe utumwani na katika ukafiri?" (Abu Daud). Mtu akizaa na mjakazi wake, basi mjakazi huyo atakuwa huru (Ibni Majah).

"Mjakazi aliyekaa kinyumba na bwana wake atahesabiwa kuwa huru, hata kama akiharibu mimba (Kashful-Ghummah). Kwa nini kulikuwa wajakazi, soma sura 4:25.

Sasa tugeukie habari za watumwa wanaotaka hati zinazoelezwa na Aya hii. Desturi hii ya kutaka hati inaitwa Mukaatabah, yaani kuandikiana mkataba. Hii ni desturi ya kuweka watumwa huru kwa lazima, iliyoamrishwa na dini ya Kiislamu. Bwana ilimbidi kumweka huru mtumwa aliyejistahilisha kuwekwa huru. Na kukata shauri kuwa amestahili kujiweka huru, haikuwa kazi ya bwana wake, bali ya serikali, kwa kuandikiana kuwa atalipa fedha sawa na uwezo wake. Wakati

wo wote mtumwa alipodai mapatano ya mkataba ilikuwa lazima bwana wake akubali, kama mtumwa huyo anayo maarifa ya kufanya kazi ya kujiweka mwenyewe, ili asiwalemee wengine kwa kumpa matumizi.

Zaidi ya hayo, serikali imeamriwa kutumia hazina yake kwa kuwakomboa watumwa pia (sura 9:60).

Kwa kufuata mafundisho ya Uislamu, Waislamu walifanya kila juhudi kukomboa watumwa kwa gharama zao wenyewe. Kwa mfano: Mtume *s.a.w* alikomboa watumwa 63; mkewe Bi Aisha, watumwa 67; Abbas, baba yake mdogo, watumwa 70; Hakim Bin Hizam 100, Abdullah Bin Omar 1,000; Abdur-Rahman Bin Auf, 30,000; Uthman Bin Afan, 20,000 katika siku moja tu ambayo aliuawa, au si hivyo angekomboa zaidi; Dhul Kila Al-Himiari, watumwa 8,000 katika siku moja. Hao wote jumla yao ni watumwa 39,000 waliokombolewa na Waislamu wachache tu (Subul-us-Salaam). Kama orodha ya masahaba wote ingepatikana, hesabu ya watumwa waliokombolewa kwa mafundisho ya Mtume s.a.w. ingeonekana kubwa ajabu.

Ikumbukwe ya kwamba mateka waliopatikana katika vita walikuwa ni wafungwa wa vita, na kwa kuwa hakukuwa magereza, na askari hawakuajiriwa, ilibidi mateka hao wawekwe kwa watu, na baadaye walipewa ruhusa kwa kujikomboa au bure. Hao mateka, ndio namna ya watumwa waliowekwa na Waislamu, nao walitendewa wema wa kila namna. Walilishwa chakula kile kile walichokula bwana na wakivishwa mavazi yale yale waliyovaa bwana zao, na wakifanya kazi za kiasi tu sawa na uwezo wao.

Mtu angeweza kuuliza swali moja. Ikiwa Islam ilikuwa na agizo la uhuru kwa watumwa, kwa nini Mtume *s.a.w.* hakutoa amri kuachwa watumwa wote mara moja?

"Jibu fupi lililo rahisi kwa swali hili ni kuwa Nabii Mtakatifu hakufanya hayo kwa sababu alikuwa rafiki wa kweli wa watumwa na alivyokusudia ilikuwa matengenezo ya kweli wala si sherehe tupu. Hakufanya lo lote lililoonekana kwa nje la urafiki kwa watumwa, lakini ambalo lilikuwa la madhara sana kwao na la hasara kwa hali njema na maendeleo ya nchi. Kila mtu wa akili aweza kuona kwa urahisi kwamba kuweka huru mara moja watumwa mamia elfu katika hali iliyokuwa imetangaa katika nchi siku zile ilikuwa kuwapoteza katika nchi hali ni wadhaifu kabisa na wasiolindwa, na hii ni hatari sana kwaona kwa nchi nzima kwa sababu nyingi wala si moja. Matokeo ya mageuko haya ya kuweka huru watumwa wote pamoja, yangekuwa hivi kwamba sehemu ya watumwa waliokombolewa wangekuwa maskini na kufa njaa, wengine wangelazimishwa, kwa sababu ya kukosa kazi, kuchagua maisha ya uhalifu, na kwa kuharibika tabia zao wangegeuka kuwa sababu ya kuleta wasiwasi mkubwa katika nchi na kwa watu wote. Mashauri ya kugeuza mara moja yangevuta nia zetu na kuonekana ya kutamanisha, lakini kwa sababu nyingi yasingethubutika kuwa bora, na mara kwa mara huleta ushawishi mbaya sana katika tabia za watu hata za maisha ya jamii ya taifa lote.

"Hivyo, Nabii Mtakatifu, aliyekuwa mwalimu wa kweli na aliyetamani kuwatendea watumwa ambayo yalikuwa yenye faida hasa kwao, hakufuta njia yo yote ya namna hiyo ambayo ingekuwa ya hasara sana kwa jamaa na kuleta madhara kuliko kuleta njema kwa watumwa." Habari zaidi juu ya watumwa, soma kitabu "Islam na Uhuru wa Watumwa."

Kabla hatujaacha maelezo haya, tuseme kidogo jambo moja. Utumwa ulioendeshwa katika Afrika, uliendeshwa kwa kadri ndogo na Waarabu na kadiri kubwa sana uliendeshwa na Wazungu. Haya ni kwa kuhusiana na Afrika nzima, si Afrika Mashariki tu. Waarabu kwa kuendesha utumwa waliasi amri ya dini yao. Hivyo tutawalaumu wale waasi, lakini hatuwezi kuilaumu dini ya Kiislamu. Maana dini ya Kiislamu iliharimisha utumwa, lakini wao wakashika watumwa na kuasi amri ya Mungu. Hivyo kosa ni la waasi, si kosa la dini ya Mungu. Hii ndiyo hakika ambayo hata mwandishi Mzungu, Mr. T. R. Batten, (Vice Principal, Makerere College, Kampala, Uganda), aliyeandika historia ya nchi hii amelazimika kuikubali. Kwanza naye alikuwa na mawazo yenye makosa juu ya jambo hili, na katika vitabu vyake vya mbele alimlaumu Mtume s.a.w. bure bila ujuzi wa kutosha, kwa kuiga maneno ya wenziwe wa Ulaya. Hapo tulimshika sana kwa hoja na

35. Na kwa yakini Tumewaterem-shieni Aya zinazoeleza waziwazi, na mfano katika wale waliopita kabla yenu, na mawaidha kwa wacha-Mungu.

وَلَقَدْ اَنْزَلْنَآ اِلَيْكُمْ اٰيٰتٍ مُّبَيِّنٰتٍ وَّمَثَلًا
مِّنَ الَّذِيْنَ خَلَوْا مِنْ قَبْلِكُمْ وَمَوْعِظَةً
لِّلْمُتَّقِيْنَ ﴿٣٥﴾ ع ١٠

dalili hata akaona ni kweli maneno yetu, na katika chapa nyingine za kitabu chake zilizofuata akabadili maneno yake, na akaandika haya: "Waislamu waliofanya biashara ya utumwa wanastahili kulaumiwa kwa kuasi amri ya Muhammad katika jambo hili" (Tropical Africa in World History, Book 1, p. 136-137).

Lakini Wazungu Wakristo kwa kushika watumwa watalaumiwa wao pamoja na dini yao. Maana, kwa nini Biblia iliweka kanuni ya kununua watumwa? Kwa nini Yesu hakusema neno la Kuwaombea uhuru watumwa waliokuwako zamani zake? Kwa nini Injili inawakazania watumwa kutii tu bila mabwana zao kukatazwa kuwafunga? Basi, si ajabu kuona ya kwamba leo Amerika kuna Waafrika 15,000,000 (milioni kumi na tano, au tuseme laki mia moja na hamsini) ambao sababu ya kufika kwao huko ni kwamba walitiwa utumwani kwenda lima mashamba ya Wakristo weupe.

Wala siyo ajabu kuona ya kwamba Kanisa lilifahamu kutia watu utmwani ndiyo ucha-Mungu. Imeandikwa, "Hata kukamata watumwa, na kufanya biashara ya watumwa, vilifahamiwa kwa yakini kabisa kuwa ni vitendo vya ucha-Mungu, vya Wakristo, kwa sababu ilionekana kufanya hivyo tu ndiyo njia iliyokuwako ya kuweza kuokoa roho za washenzi" (Christianity in Africa, p. 125, kilichotungwa na padre wa Kijerumani, aitwaye Diedrich Westermann). Ukurasa 126 wa kitabu hicho, ameandika, "Hapa pia tunatoa uhusiano uchukizao baina ya Kanisa na utumwa: nyumba ya Majeshi watawa katika Sao Paulo de Loanda, ilikuwa na watumwa 12,000 (kumi na mbili elfu), na shehena ya watumwa waliopelekwa Brazil, hawakuruhusiwa kuitoka nchi ya jadi yao milele mpaka walipotiwa baraka na Askofu wa Loanda."

Kadhalika kitabu kiitwacho, "The New Congo" kinaeleza ya kwamba mapema katika mwaka 1500 kambi ya watumwa ilipigwa na Wakristo katika uingilio wa mto Kongo, na kwa miaka 350 wakaendesha kukamata watumwa ili kuokoa roho zao ingawa miili yao ipate mateso utumwani. Na mahali pengine tunasoma ya kuwa "mapadre hawakulalamika kamwe kuilaumu biashara hii ya utumwa ingawa iko kinyume cha mafundisho ya kanisa lao, maana waliipatia faida" (E. G. Ravenstein, The Hakluyt Society, London);

Ama Wazungu kama Abraham Lincoln, na mabwana wengine waliofanya bidii kukataza utumwa huko Amerika na huku, na kwingineko, wanastahili kushukuriwa, lakini hawakufanya hivyo kwa kuwa ndiyo dini ya Kikristo imewafunza, la. Bali ni kwa sababu ya roho zao wenyewe za kiutu, waila Ukristo usingekataza. Na ungekatazaje hali kanisa lenyewe lilikuwa limeshughulika katika kazi ya kuwinda watumwa?

Msiwashurutishe vijana wenu wa kike kufanya ukahaba, Mradi hapa unaweza kuwa namna mbili: (1) Baadhi ya watu hawawaposi binti zao kwa sababu ya tamaa ya kupatikana wachumba wenye mali. Hata inakuwa binti wale, kwa kuwa wamekua, wanaanza kushawishika kuingia katika maovu. (2) Baadhi ya watu hawawazuii vijana wao wa kike kufanya ukahaba maana wanapata faida katika vitu wanavyohongwa, na wanaona kama wanasaidiwa katika matumizi, au wanawashurutisha wanawake kufanya ukahaba ili wapate mali. Basi desturi hizi zote ni mbaya sana na zimekatazwa na Aya hii.

FUNGU 5

اَللّٰهُ نُوْرُ السَّمٰوٰتِ وَالْاَرْضِ ؕ مَثَلُ
نُوْرِهٖ كَمِشْكٰوةٍ فِيْهَا مِصْبَاحٌ ؕ اَلْمِصْبَاحُ
فِيْ زُجَاجَةٍ ؕ اَلزُّجَاجَةُ كَاَنَّهَا كَوْكَبٌ
دُرِّيٌّ يُّوْقَدُ مِنْ شَجَرَةٍ مُّبٰرَكَةٍ زَيْتُوْنَةٍ
لَّا شَرْقِيَّةٍ وَّلَا غَرْبِيَّةٍ ۙ يَّكَادُ زَيْتُهَا
يُضِيْٓءُ وَلَوْ لَمْ تَمْسَسْهُ نَارٌ ؕ نُوْرٌ عَلٰى
نُوْرٍ ؕ يَهْدِى اللّٰهُ لِنُوْرِهٖ مَنْ يَّشَآءُ ؕ
وَيَضْرِبُ اللّٰهُ الْاَمْثَالَ لِلنَّاسِ ؕ وَاللّٰهُ
بِكُلِّ شَيْءٍ عَلِيْمٌ ۙ﴿۳۶﴾

36. Allah ni nuru ya mbingu na ardhi; mfano wa nuru Yake ni kama kishubaka kilichomo ndani ya taa: taa ile imo katika tungi: tungi lile ni kama nyota ing'aayo, inayowashwa katika mti uliobarikiwa wa mzeituni, usio wa mashariki wala wa magharibi; ni karibu mafuta yake kung'aa ingawa moto haujayagusa - nuru juu ya nuru - Allah Humwongoza kwenye nuru Yake Amtakaye, na Allah Hupiga mifano kwa watu; na Allah ni Mjuzi wa kila kitu.

فِيْ بُيُوْتٍ اَذِنَ اللّٰهُ اَنْ تُرْفَعَ وَيُذْكَرَ فِيْهَا
اسْمُهٗ ۙ يُسَبِّحُ لَهٗ فِيْهَا بِالْغُدُوِّ وَالْاٰصَالِ ۙ﴿۳۷﴾

37. Katika nyumba ambazo Allah Ameruhusu zinyanyuliwe, na humo lita - jwe jina Lake; humtukuza humo asubuhi na jioni,

رِجَالٌ ۙ لَّا تُلْهِيْهِمْ تِجَارَةٌ وَّلَا بَيْعٌ عَنْ
ذِكْرِ اللّٰهِ وَاِقَامِ الصَّلٰوةِ وَاِيْتَآءِ الزَّكٰوةِ ۙ۬
يَخَافُوْنَ يَوْمًا تَتَقَلَّبُ فِيْهِ الْقُلُوْبُ
وَالْاَبْصَارُ ۙ﴿۳۸﴾

38. Watu (adhimu) ambao haiwasahaulishi biashara wala uchumi katika kumkumbuka Allah na kusimamisha Sala na kutoa Zaka, wanaiogopa Siku ambayo mioyo itapinduka na macho (pia);

Aya 36. Aya hii inaonyesha ya kuwa kila kitu kinachoonekana duniani na mbinguni ni maonyesho ya nuru ya Allah.

Aya 37. *Zinyanyuliwe,* sio mradi wake ya kuwa nyumba hizi zilipandishwa mbinguni, bali maana yake zilitukuzwa. Neno hili hili la kunyanyua lilitumiwa kwa ajili ya Nabii Isa ya kwamba hakulaaniwa kama walivyomtangaza Mayahudi, ila alitukuzwa; lakini watu wasio na ujuzi wameanza kudhania maana yake ni kupeleka mbinguni.

Aya 38. Hii iliyoelezwa hapa ndiyo hali ya masahaba wa Mtume *s.a.w.* Wao ingawa walifanya biashara na kazi zingine, lakini hazikuwasahaulisha mambo ya ibada na Zaka na kumkumbuka Allah. Ukamilifu wa mtu si katika kuacha kazi, ambazo ndizo humtengenezea maisha yake ya dunia, bali kuendesha kazi zake na kumkumbuka Mungu zaidi.

لِيَجْزِيَهُمُ اللّٰهُ اَحْسَنَ مَا عَمِلُوْا وَيَزِيْدَهُمْ مِّنْ فَضْلِهٖ ؕ وَاللّٰهُ يَرْزُقُ مَنْ يَّشَآءُ بِغَيْرِ حِسَابٍ ﴿٣٩﴾

39. Ili Allah Awalipe mazuri ya yale waliyoyafanya, na kuwazidishia katika fadhili Zake; na Allah Humruzuku Amtakaye pasipo hesabu.

وَالَّذِيْنَ كَفَرُوْٓا اَعْمَالُهُمْ كَسَرَابٍۭ بِقِيْعَةٍ يَّحْسَبُهُ الظَّمْاٰنُ مَآءً ؕ حَتّٰٓى اِذَا جَآءَهٗ لَمْ يَجِدْهُ شَيْـًٔا وَّوَجَدَ اللّٰهَ عِنْدَهٗ فَوَفّٰىهُ حِسَابَهٗ ؕ وَاللّٰهُ سَرِيْعُ الْحِسَابِ ﴿٤٠﴾

40. Na wale waliokufuru, vitendo vyao ni kama mazigazi jangwani, mwenye kiu huyadhani ni maji; hata ayafikiapo hapati cho chote, na humkuta Allah hapo, naye Humpa hesabu yake sawasawa; na Allah ni Mwepesi wa kuhesabu.

اَوْ كَظُلُمٰتٍ فِيْ بَحْرٍ لُّجِّيٍّ يَّغْشٰىهُ مَوْجٌ مِّنْ فَوْقِهٖ مَوْجٌ مِّنْ فَوْقِهٖ سَحَابٌ ؕ ظُلُمٰتٌۢ بَعْضُهَا فَوْقَ بَعْضٍ ؕ اِذَآ اَخْرَجَ يَدَهٗ لَمْ يَكَدْ يَرٰىهَا ؕ وَمَنْ لَّمْ يَجْعَلِ اللّٰهُ لَهٗ نُوْرًا فَمَا لَهٗ مِنْ نُّوْرٍ ﴿٤١﴾ ع

41. Au ni kama giza katika bahari yenye lindi; huifunika mawimbi juu yake mawimbi, juu yake kuna mawingu, giza hili juu ya hili; anapoutoa mkono wake hawezi kuuona; na ambaye Allah Hakumjaalia nuru, basi huyo hana nuru.

FUNGU 6

اَلَمْ تَرَ اَنَّ اللّٰهَ يُسَبِّحُ لَهٗ مَنْ فِى السَّمٰوٰتِ وَالْاَرْضِ وَالطَّيْرُ صٰٓفّٰتٍ ؕ كُلٌّ قَدْ عَلِمَ صَلَاتَهٗ وَتَسْبِيْحَهٗ ؕ وَاللّٰهُ عَلِيْمٌۢ بِمَا يَفْعَلُوْنَ ﴿٤٢﴾

42. Je, huoni kwamba Allah vinamtukuza vilivyomo mbinguni na ardhini, na ndege kwa kukunjua mbawa zao? Kila (mmoja wao) amekwisha jua sala yake na tasbihi yake; na Allah ni Mjuzi wa (yale) wanayoyafanya.

وَلِلّٰهِ مُلْكُ السَّمٰوٰتِ وَالْاَرْضِ ۚ وَاِلَى اللّٰهِ الْمَصِيْرُ ﴿٤٣﴾

43. Na ni wa Allah ufalme wa mbingu na ardhi, na kwa Allah ndiko marejeo.

اَلَمْ تَرَ اَنَّ اللّٰهَ يُزْجِىْ سَحَابًا ثُمَّ يُؤَلِّفُ بَيْنَهٗ ثُمَّ يَجْعَلُهٗ رُكَامًا فَتَرَى الْوَدْقَ يَخْرُجُ مِنْ خِلٰلِهٖ ۚ وَيُنَزِّلُ مِنَ السَّمَآءِ مِنْ جِبَالٍ فِيْهَا مِنْۢ بَرَدٍ فَيُصِيْبُ بِهٖ مَنْ يَّشَآءُ

44. Je, huoni ya kwamba Allah Anayaendesha mawingu, kisha Huyakusanya pamoja, kisha Huyalundika, kisha unaona mvua ikitoka katikati yake; Naye Huteremsha kutoka juu, yaani kwenye milima ya mawingu, mvua ya mawe, kisha Humfikishia

وَيَصْرِفُهٗ عَنْ مَّنْ يَّشَآءُ ؕ يَكَادُ سَنَا بَرْقِهٖ يَذْهَبُ بِالْاَبْصَارِ ؕ﴿۴۴﴾

Amtakaye na kumwepusha nayo Amtakaye; karibu mwanga wa umeme wake unyakue kuona (kwao).

يُقَلِّبُ اللّٰهُ الَّيْلَ وَالنَّهَارَ ؕ اِنَّ فِيْ ذٰلِكَ لَعِبْرَةً لِّاُولِي الْاَبْصَارِ ﴿۴۵﴾

45. Allah Hubadilisha usiku na mchana; bila shaka katika hayo imo dalili kwa watu wenye busara.

وَاللّٰهُ خَلَقَ كُلَّ دَآبَّةٍ مِّنْ مَّآءٍ ۚ فَمِنْهُمْ مَّنْ يَّمْشِيْ عَلٰى بَطْنِهٖ ۚ وَمِنْهُمْ مَّنْ يَّمْشِيْ عَلٰى رِجْلَيْنِ ۚ وَمِنْهُمْ مَّنْ يَّمْشِيْ عَلٰۤى اَرْبَعٍ ؕ يَخْلُقُ اللّٰهُ مَا يَشَآءُ ؕ اِنَّ اللّٰهَ عَلٰى كُلِّ شَيْءٍ قَدِيْرٌ ﴿۴۶﴾

46. Na Allah Alimwumba kila mnyama kwa maji: wengine wao huenda kwa matumbo yao, na wengine wao huenda kwa miguu miwili, na wengine wao huenda kwa minne; Allah Huumba Ayatakayo. Hakika Allah Anao uwezo juu ya kila kitu.

لَقَدْ اَنْزَلْنَاۤ اٰيٰتٍ مُّبَيِّنٰتٍ ؕ وَاللّٰهُ يَهْدِيْ مَنْ يَّشَآءُ اِلٰى صِرَاطٍ مُّسْتَقِيْمٍ ﴿۴۷﴾

47. Kwa yakini Tumeteremsha Aya zinazobainisha; na Allah Humwongoza Amtakaye kwenye njia iliyonyooka.

وَيَقُوْلُوْنَ اٰمَنَّا بِاللّٰهِ وَبِالرَّسُوْلِ وَاَطَعْنَا ثُمَّ يَتَوَلّٰى فَرِيْقٌ مِّنْهُمْ مِّنْۢ بَعْدِ ذٰلِكَ ؕ وَمَاۤ اُولٰٓئِكَ بِالْمُؤْمِنِيْنَ ﴿۴۸﴾

48. Na wanasema: Tumemwamini Allah na Mtume, na tunatii; kisha hugeuka kundi moja kati yao baada ya hayo; na hao si waaminio.

وَاِذَا دُعُوْۤا اِلَى اللّٰهِ وَرَسُوْلِهٖ لِيَحْكُمَ بَيْنَهُمْ اِذَا فَرِيْقٌ مِّنْهُمْ مُّعْرِضُوْنَ ﴿۴۹﴾

49. Na wanapoitwa kwa Allah na Mtume Wake ili Awahukumu baina yao, ndipo kundi moja miongoni mwao linajitenga.

وَاِنْ يَّكُنْ لَّهُمُ الْحَقُّ يَاْتُوْۤا اِلَيْهِ مُذْعِنِيْنَ ؕ﴿۵۰﴾

50. Na kama ikiwa haki ni yao, wanamfikia kwa kutii.

اَفِيْ قُلُوْبِهِمْ مَّرَضٌ اَمِ ارْتَابُوْۤا اَمْ يَخَافُوْنَ اَنْ يَّحِيْفَ اللّٰهُ عَلَيْهِمْ وَرَسُوْلُهٗ ؕ بَلْ اُولٰٓئِكَ هُمُ الظّٰلِمُوْنَ ﴿۵۰﴾ ع ۱۳

51. Je, wanayo maradhi katika mioyo yao, au wanaona shaka, au wanaogopa ya kuwa Atawadhulumu Allah na Mtume Wake? Bali hao ndio wadhalimu.

FUNGU 7

اِنَّمَا كَانَ قَوْلَ الْمُؤْمِنِيْنَ اِذَا دُعُوْٓا
اِلَى اللّٰهِ وَ رَسُوْلِهٖ لِيَحْكُمَ بَيْنَهُمْ
اَنْ يَّقُوْلُوْا سَمِعْنَا وَ اَطَعْنَا ؕ وَ اُولٰٓئِكَ
هُمُ الْمُفْلِحُوْنَ ﴿۵۲﴾

52. Haiwi kauli ya waaminio wanapoitwa kwa Allah na Mtume Wake ili Ahukumu baina yao, ila kusema: Tunasikia na tunakubali; na hao ndio wapatao ufaulu.

وَمَنْ يُّطِعِ اللّٰهَ وَ رَسُوْلَهٗ وَ يَخْشَ اللّٰهَ
وَ يَتَّقْهِ فَاُولٰٓئِكَ هُمُ الْفَآئِزُوْنَ ﴿۵۳﴾

53. Na anayemtii Allah na Mtume Wake, na kumnyenyekea Allah na kumwogopa, basi hao ndio watakaofuzu.

وَاَقْسَمُوْا بِاللّٰهِ جَهْدَ اَيْمَانِهِمْ لَئِنْ
اَمَرْتَهُمْ لَيَخْرُجُنَّ ؕ قُلْ لَّا تُقْسِمُوْا ۚ
طَاعَةٌ مَّعْرُوْفَةٌ ؕ اِنَّ اللّٰهَ خَبِيْرٌۢ بِمَا
تَعْمَلُوْنَ ﴿۵۴﴾

54. Na walimwapia Allah kwa kiapo chao cha nguvu, ya kwamba ukiwaamrisha, bila shaka wataondoka. Sema: Msiape; utii wa kawaida (ndio unaotakiwa) Hakika Allah Anazo habari za mnayoyatenda.

قُلْ اَطِيْعُوا اللّٰهَ وَاَطِيْعُوا الرَّسُوْلَ ۚ فَاِنْ
تَوَلَّوْا فَاِنَّمَا عَلَيْهِ مَا حُمِّلَ وَعَلَيْكُمْ مَّا
حُمِّلْتُمْ ؕ وَاِنْ تُطِيْعُوْهُ تَهْتَدُوْا ؕ وَمَا
عَلَى الرَّسُوْلِ اِلَّا الْبَلٰغُ الْمُبِيْنُ ﴿۵۵﴾

55. Sema: Mtiini Allah na mtiini Mtume; na kama mkikengeuka, basi aliyolazimishwa yeye ni juu yake, na ni juu yenu mliyolazimishwa ninyi: na kama mkimtii mtaongoka; si vingine juu ya Mtume ila kufikisha (ujumbe) waziwazi.

وَعَدَ اللّٰهُ الَّذِيْنَ اٰمَنُوْا مِنْكُمْ وَعَمِلُوا
الصّٰلِحٰتِ لَيَسْتَخْلِفَنَّهُمْ فِى الْاَرْضِ كَمَا
اسْتَخْلَفَ الَّذِيْنَ مِنْ قَبْلِهِمْ ۪ وَ لَيُمَكِّنَنَّ
لَهُمْ دِيْنَهُمُ الَّذِى ارْتَضٰى لَهُمْ
وَلَيُبَدِّلَنَّهُمْ مِّنْۢ بَعْدِ خَوْفِهِمْ اَمْنًا ؕ
يَعْبُدُوْنَنِىْ لَا يُشْرِكُوْنَ بِىْ شَيْـًٔا ؕ وَمَنْ
كَفَرَ بَعْدَ ذٰلِكَ فَاُولٰٓئِكَ هُمُ الْفٰسِقُوْنَ ﴿۵۶﴾

56. Allah Amewaahidi wale walioamini miongoni mwenu na kufanya vitendo vizuri, bila shaka Atawafanya makhalifa katika ardhi kama Alivyowafanya makhalifa wale wa kabla yao, na kwa yakini Atawaimarishia dini yao Aliyowapendelea, na Atawabadilishia amani baada ya hofu yao. Wataniabudu, hawatanishirikisha na cho chote. Na atakayekufuru baada ya hayo, basi hao ndio wavunjao amri.

Aya 56. *Atawafanya Makhalifa katika ardhi.* Aya hii inaeleza ya kuwa Allah atainua makhalifa katika umati huu kama vile alivyoinua makhalifa katika umati wa Musa. Na

57. Na simamisheni Sala na toeni Zaka na mtiini Mtume, ili mrehemewe.

وَاَقِيْمُوا الصَّلٰوةَ وَاٰتُوا الزَّكٰوةَ وَاَطِيْعُوا الرَّسُوْلَ لَعَلَّكُمْ تُرْحَمُوْنَ ﴿٥٧﴾

58. Msiwadhanie wale waliokufuru kwamba wataponyoka katika ardhi; na makao yao ni Moto; na marudio yao bila shaka ni mabaya.

لَا تَحْسَبَنَّ الَّذِيْنَ كَفَرُوْا مُعْجِزِيْنَ فِي الْاَرْضِ ۚ وَمَاْوٰىهُمُ النَّارُ ؕ وَلَبِئْسَ الْمَصِيْرُ ﴿٥٨﴾ ع ۴

FUNGU 8

59. Enyi mlioamini! wawaombeni ruhusa (ya kuingia ndani ya vyumba vyenu vya kulala) wale iliyowamiliki mikono yenu ya kuume, na wale wasiofikia balehe miongoni mwenu, katika nyakati tatu: kabla ya Sala ya Alfajiri na mnapovua nguo zenu (za ziada nyakati za) adhuhuri, na baada ya Sala ya Isha; hizi ni nyakati tatu za faragha kwenu. Si dhambi kwenu wala kwao, mbali ya nyakati hizo (kutembeleana bila ruhusa maalum); mara nyingi huwa mnatembeleana. Hivyo ndivyo Allah Anavyowaelezeni Aya, na Allah ni Mjuzi, Mwenye hekima.

يٰۤاَيُّهَا الَّذِيْنَ اٰمَنُوْا لِيَسْتَاْذِنْكُمُ الَّذِيْنَ مَلَكَتْ اَيْمَانُكُمْ وَالَّذِيْنَ لَمْ يَبْلُغُوا الْحُلُمَ مِنْكُمْ ثَلٰثَ مَرّٰتٍ ؕ مِنْ قَبْلِ صَلٰوةِ الْفَجْرِ وَحِيْنَ تَضَعُوْنَ ثِيَابَكُمْ مِّنَ الظَّهِيْرَةِ وَمِنْۢ بَعْدِ صَلٰوةِ الْعِشَآءِ ۚ ثَلٰثُ عَوْرٰتٍ لَّكُمْ ؕ لَيْسَ عَلَيْكُمْ وَلَا عَلَيْهِمْ جُنَاحٌۢ بَعْدَهُنَّ ؕ طَوّٰفُوْنَ عَلَيْكُمْ بَعْضُكُمْ عَلٰى بَعْضٍ ؕ كَذٰلِكَ يُبَيِّنُ اللّٰهُ لَكُمُ الْاٰيٰتِ ؕ وَاللّٰهُ عَلِيْمٌ حَكِيْمٌ ﴿٥٩﴾

60. Na watoto watakapobalehe miongoni mwenu, basi waombe ruhusa kama walivyoomba ruhusa wale wa kabla yao. Hivyo ndivyo Allah Anavyokubainishieni Aya Zake, na Allah ni Mjuzi, Mwenye hekima.

وَاِذَا بَلَغَ الْاَطْفَالُ مِنْكُمُ الْحُلُمَ فَلْيَسْتَاْذِنُوْا كَمَا اسْتَاْذَنَ الَّذِيْنَ مِنْ قَبْلِهِمْ ؕ كَذٰلِكَ يُبَيِّنُ اللّٰهُ لَكُمْ اٰيٰتِهٖ ؕ وَاللّٰهُ عَلِيْمٌ حَكِيْمٌ ﴿٦٠﴾

61. Na kwa wanawake wakongwe ambao wamevuka umri wa kuolewa, hakuna lawama juu yao kutandua

وَالْقَوَاعِدُ مِنَ النِّسَآءِ الّٰتِيْ لَا يَرْجُوْنَ نِكَاحًا فَلَيْسَ عَلَيْهِنَّ جُنَاحٌ اَنْ يَّضَعْنَ

pia inaeleza ya kuwa makhalifa hao watafanya kazi ya kuipa nguvu dini, na Waislamu watakaowakataa watakuwa wavunjao amri. Na kwa kuwa Nabii Isa alikuwa Khalifa wa Nabii Musa miaka 1300 baada yake, kukamilisha mfano huo, Allah amemleta Seyidna Ahmad kuwa Khalifa baada ya Mtume *s.a.w.* miaka 1300 ili kusimamisha Sheria ya Kiislamu. Waidha Aya hii inathibitisha ya kuwa Seyidna Abu Bakar na seyidna Umar na Seyidna Uthman na Seyidna Ali wote walikuwa Makhalifa wa kweli na walipata msaada kwa Allah, na kila mmoja wao alikuwa paa la Uislamu (Mungu awe radhi nao).

Aya 61. Wanawake wakaao, yaani wanawake wazee.

ثِيَابَهُنَّ غَيْرَ مُتَبَرِّجٰتٍ بِزِيْنَةٍ ؕ وَاَنْ
يَّسْتَعْفِفْنَ خَيْرٌ لَّهُنَّ ؕ وَاللّٰهُ سَمِيْعٌ
عَلِيْمٌ ﴿٦٠﴾

mitandio yao lakini wasionyeshe uzuri wao kwa makusudi. Na kama wakihiari kuchukua hadhari zaidi katika kulinda utakatifu wao ni vyema zaidi kwa ajili yao. Na Allah ni Asikiaye Ajuyae.

لَيْسَ عَلَى الْاَعْمٰى حَرَجٌ وَّلَا عَلَى
الْاَعْرَجِ حَرَجٌ وَّلَا عَلَى الْمَرِيْضِ
حَرَجٌ وَّلَا عَلٰٓى اَنْفُسِكُمْ اَنْ تَاْكُلُوْا مِنْ
بُيُوْتِكُمْ اَوْ بُيُوْتِ اٰبَآئِكُمْ اَوْ بُيُوْتِ
اُمَّهٰتِكُمْ اَوْ بُيُوْتِ اِخْوَانِكُمْ اَوْ بُيُوْتِ
اَخَوٰتِكُمْ اَوْ بُيُوْتِ اَعْمَامِكُمْ اَوْ بُيُوْتِ
عَمّٰتِكُمْ اَوْ بُيُوْتِ اَخْوَالِكُمْ اَوْ بُيُوْتِ
خٰلٰتِكُمْ اَوْ مَا مَلَكْتُمْ مَّفَاتِحَهٗٓ اَوْ
صَدِيْقِكُمْ ؕ لَيْسَ عَلَيْكُمْ جُنَاحٌ اَنْ
تَاْكُلُوْا جَمِيْعًا اَوْ اَشْتَاتًا ؕ فَاِذَا دَخَلْتُمْ
بُيُوْتًا فَسَلِّمُوْا عَلٰٓى اَنْفُسِكُمْ تَحِيَّةً مِّنْ
عِنْدِ اللّٰهِ مُبٰرَكَةً طَيِّبَةً ؕ كَذٰلِكَ يُبَيِّنُ
اللّٰهُ لَكُمُ الْاٰيٰتِ لَعَلَّكُمْ تَعْقِلُوْنَ ﴿٦١﴾ ع

62. Si vibaya kwa kipofu, wala si vibaya kwa kilema, wala si vibaya kwa mgonjwa, wala kwenu, kama mkila katika nyumba zenu, au nyumba za baba zenu, au nyumba za mama zenu, au nyumba za ndugu zenu, au nyumba za dada zenu, au nyumba za amu zenu, au nyumba za shangazi zenu, au nyumba za wajomba zenu, au nyumba za dada za mama zenu, au za wale mliowashikia funguo zao, au ya nyumba ile mnayomiliki funguo zake au ya nyumba za rafiki zenu. Si vibaya kwenu kama mkila pamoja au mbalimbali. Na mnapoingia katika majumba, basi mtoleane salamu, ni hidaya itokayo kwa Allah, yenye baraka, njema. Hivyo ndivyo Allah Anavyowabainishieni Aya ili mpate kutumia akili.

FUNGU 9

اِنَّمَا الْمُؤْمِنُوْنَ الَّذِيْنَ اٰمَنُوْا بِاللّٰهِ
وَرَسُوْلِهٖ وَاِذَا كَانُوْا مَعَهٗ عَلٰٓى اَمْرٍ
جَامِعٍ لَّمْ يَذْهَبُوْا حَتّٰى يَسْتَاْذِنُوْهُ ؕ
اِنَّ الَّذِيْنَ يَسْتَاْذِنُوْنَكَ اُولٰٓئِكَ

63. Waaminio wa kweli ni wale tu waliomwamini Allah na Mtume Wake; na wanapokuwa pamoja naye kwa jambo linalohusiana na wote, hawaondoki mpaka wamwombe ruhusa. Kwa yakini wale wanaokuomba ruhusa,

Aya 62. *Mnapoingia katika majumba, basi mtoleane salamu.* Ni jambo la kustaajabisha sana kuona Waislamu wengi mno hawashiki sheria hii, na wakiingia majumbani mwao wanaingia kimya. Hii si desturi nzuri. Watu wa nyumbani wana haki ya kuombewa salama kama vile walivyo na haki watu wengine.

Aya 63. *Hawaondoki mpaka wamwombe ruhusa.* Aya hii inafundisha adabu ya watu wanaokaa katika umoja na wana mkubwa wao. Wakiwa katika kazi au mashauri hawaondoki ovyo ila kwanza hutaka ruhusa.

الَّذِيْنَ يُؤْمِنُوْنَ بِاللّٰهِ وَ رَسُوْلِهٖ ۚ
فَاِذَا اسْتَاْذَنُوْكَ لِبَعْضِ شَاْنِهِمْ فَاْذَنْ
لِّمَنْ شِئْتَ مِنْهُمْ وَاسْتَغْفِرْ لَهُمُ اللّٰهَ ؕ
اِنَّ اللّٰهَ غَفُوْرٌ رَّحِيْمٌ ﴿٦٢﴾

hao ndio wanaomwamini Allah na Mtume Wake. Na watakapokuomba ruhusa kwa ajili ya baadhi ya kazi zao, basi mruhusu umtakaye miongoni mwao, na uwaombee ghofira kwa Allah. Hakika Allah ni Msamehevu, Mrehemevu.

لَا تَجْعَلُوْا دُعَآءَ الرَّسُوْلِ بَيْنَكُمْ
كَدُعَآءِ بَعْضِكُمْ بَعْضًا ؕ قَدْ يَعْلَمُ اللّٰهُ
الَّذِيْنَ يَتَسَلَّلُوْنَ مِنْكُمْ لِوَاذًا ۚ
فَلْيَحْذَرِ الَّذِيْنَ يُخَالِفُوْنَ عَنْ اَمْرِهٖۤ
اَنْ تُصِيْبَهُمْ فِتْنَةٌ اَوْ يُصِيْبَهُمْ
عَذَابٌ اَلِيْمٌ ﴿٦٣﴾

64. Msifanye wito wa Mtume baina yenu kama wito wa ninyi kwa ninyi. Hakika Allah Anawajua miongoni mwenu wale waondokao kwa utoro wakijificha. Basi wajihadhari wale wanaokaidi amri Yake, isije ukawapata msiba au ikawafikia adhabu iumizayo.

اَلَاۤ اِنَّ لِلّٰهِ مَا فِي السَّمٰوٰتِ وَ الْاَرْضِ ؕ
قَدْ يَعْلَمُ مَاۤ اَنْتُمْ عَلَيْهِ ؕ وَ يَوْمَ
يُرْجَعُوْنَ اِلَيْهِ فَيُنَبِّئُهُمْ بِمَا عَمِلُوْا ؕ
وَ اللّٰهُ بِكُلِّ شَيْءٍ عَلِيْمٌ ﴿٦٤﴾ ع ١٥

65. Sikilizeni! Ni vyake vilivyomo mbinguni na ardhini. Bila shaka Anayajua mliyo nayo. Na siku watakaporudishwa Kwake Atawaambia waliyoyafanya. Na Allah ni Mjuzi wa kila kitu.

Aya 64. *Wito wa Mtume.* Yaani, kama Mtume anamwita mtu, wito huo unakuwa na thamni zaidi, na siyo sawa na wito wanaoitwa na mtu mwingine. Pili watu wasiwe wakimwita Mtume pasipo adabu kama vile wanavyoitana wao kwa wao. Na mwisho wa Aya hii unaonyesha ya kuwa kama watu hawatashika maagizo haya hawatakuwa salama, bali yumkini iwafikie adhabu na fitina kubwa.

سُوْرَةُ الْفُرْقَانِ مَكِّيَّةٌ وَّ هِيَ مَعَ الْبَسْمَلَةِ ثَمَانٍ وَّ سَبْعُوْنَ اٰيَةً وَّ سِتَّةُ رُكُوْعَاتٍ

25. SURA AL-FURQAAN

Imeteremshwa Makka

Ina mafungu 6 na Aya 78 pamoja na Bismillahi

بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ ①

1. Kwa jina la Allah, Mwingi wa rehema, Mwingi wa ukarimu.

تَبٰرَكَ الَّذِيْ نَزَّلَ الْفُرْقَانَ عَلٰى عَبْدِهٖ لِيَكُوْنَ لِلْعٰلَمِيْنَ نَذِيْرَا ۙ ②

2. Mwenye baraka ni Yule Aliyeteremsha Furkani kwa Mtumishi Wake ili awe Mwonyaji kwa walimwengu.

الَّذِيْ لَهٗ مُلْكُ السَّمٰوٰتِ وَالْاَرْضِ وَلَمْ يَتَّخِذْ وَلَدًا وَّلَمْ يَكُنْ لَّهٗ شَرِيْكٌ فِي الْمُلْكِ وَخَلَقَ كُلَّ شَيْءٍ فَقَدَّرَهٗ تَقْدِيْرًا ③

3. Ambaye ni Wake ufalme wa mbingu na ardhi, wala Hakushika mtoto wala hana mshirika katika ufalme, na Akakiumba kila kitu, na Akakikadiria kipimo.

وَاتَّخَذُوْا مِنْ دُوْنِهٖٓ اٰلِهَةً لَّا يَخْلُقُوْنَ شَيْـًٔا وَّهُمْ يُخْلَقُوْنَ وَلَا يَمْلِكُوْنَ لِاَنْفُسِهِمْ ضَرًّا وَّلَا نَفْعًا وَّلَا يَمْلِكُوْنَ مَوْتًا وَّلَا حَيٰوةً وَّلَا نُشُوْرًا ④

4. Na wakashika badala Yake miungu ambao hawaumbi cho chote hali wao wanaumbwa, wala hawajimilikii dhara wala nufaa, wala hawamiliki mauti wala uhai wala ufufuo.

وَقَالَ الَّذِيْنَ كَفَرُوْٓا اِنْ هٰذَآ اِلَّآ اِفْكُ ۨ افْتَرٰىهُ وَاَعَانَهٗ عَلَيْهِ قَوْمٌ اٰخَرُوْنَ ۚ فَقَدْ جَآءُوْ ظُلْمًا وَّزُوْرًا ۚ ⑤

5. Na wakasema wale waliokufuru: Sio huu ila ni uzushi aliouzusha, na wanamsaidia juu yake watu wengine. Basi wameleta dhuluma na uwongo.

Sura hii nzima ni moja katika za mwanzo kushuka Makka na si sawa kusema kuwa Aya 69 - 71 zilishuka Madina kama inavyoonekana waziwazi katika sura yenyewe. Bishara zilizoshuka nyuma zilizomo katika sura iliyopita zinazoeleza kuwa ufalme wa dini ya Kiislamu utasimama, zinafuatwa na bishara iliyotangulia ya kipambanuo iliyomo katika sura hii ya kuwa kweli na uwongo vitapambanuliwa kwa namna ambayo kila jicho litaweza kuona.

Aya 2. *Furqaan.* Neno hili ni jina la Qur'an, na pia ni jina la sura hii. Maana ya neno hili ni kipambanuo baina ya kweli na batili, yaani kwa kusoma Qur'an kwa fikira mtu anapata nuru iwezayo kumsaidia kupambanua baina ya kweli na uwongo.

Awe Mwonyaji kwa walimwengu. Qur'an tu ndicho Kitabu kinachodai kuwa Islam imeletwa kwa ajili ya dunia nzima. Hakuna dini nyingine iliyodai haya. Yesu anakiri kuwa hakutumwa isipokuwa kwa kondoo waliopotea wa nyumba ya Israeli (Mattayo 15:24).

وَقَالُوْٓا اَسَاطِيْرُ الْاَوَّلِيْنَ اكْتَتَبَهَا فَهِيَ تُمْلٰى عَلَيْهِ بُكْرَةً وَّاَصِيْلًا ۝٦

6. Na wakasema: Ni visa vya (watu) wa zamani alivyoviandika, navyo anavisoma asubuhi na jioni.

قُلْ اَنْزَلَهُ الَّذِيْ يَعْلَمُ السِّرَّ فِي السَّمٰوٰتِ وَالْاَرْضِ ۭ اِنَّهٗ كَانَ غَفُوْرًا رَّحِيْمًا ۝٧

7. Sema: Ameyateremsha Yule Ajuaye siri za mbinguni na ardhini; bila shaka Yeye ni Msamehevu, Mrehemevu.

وَقَالُوْا مَالِ هٰذَا الرَّسُوْلِ يَاْكُلُ الطَّعَامَ وَيَمْشِيْ فِي الْاَسْوَاقِ ۭ لَوْلَآ اُنْزِلَ اِلَيْهِ مَلَكٌ فَيَكُوْنَ مَعَهٗ نَذِيْرًا ۝٨

8. Na wakasema: Mtume gani huyu anayekula chakula na anatembea masokoni! Mbona hakuteremshiwa Malaika awe Mwonyaji pamoja naye?

اَوْ يُلْقٰٓى اِلَيْهِ كَنْزٌ اَوْ تَكُوْنُ لَهٗ جَنَّةٌ يَّاْكُلُ مِنْهَا ۭ وَقَالَ الظّٰلِمُوْنَ اِنْ تَتَّبِعُوْنَ اِلَّا رَجُلًا مَّسْحُوْرًا ۝٩

9. Au ateremshiwe hazina au iwe kwake bustani ale katika hiyo? Na wadhalimu wakasema: Ninyi hamumfuati ila mtu aliyelogwa.

اُنْظُرْ كَيْفَ ضَرَبُوْا لَكَ الْاَمْثَالَ فَضَلُّوْا فَلَا يَسْتَطِيْعُوْنَ سَبِيْلًا ۝١٠ ع ١٠

10. Tazama jinsi wanavyokupigia mfano, basi wamepotea wala hawataweza (kushika) njia.

FUNGU 2

تَبٰرَكَ الَّذِيْٓ اِنْ شَاۗءَ جَعَلَ لَكَ خَيْرًا مِّنْ ذٰلِكَ جَنّٰتٍ تَجْرِيْ مِنْ تَحْتِهَا الْاَنْهٰرُ ۙ وَيَجْعَلْ لَّكَ قُصُوْرًا ۝١١

11. Mwenye baraka ni Yule Ambaye Akitaka Atakufanyia bora kuliko hivyo - Bustani zipitazo mito ndani yake na Akujaalie majumba ya kifalme.

بَلْ كَذَّبُوْا بِالسَّاعَةِ ۣ وَاَعْتَدْنَا لِمَنْ كَذَّبَ بِالسَّاعَةِ سَعِيْرًا ۝١٢

12. Bali waliikadhibisha saa, na Tumemwandalia aikadhibishaye saa, Moto uwakao.

اِذَا رَاَتْهُمْ مِّنْ مَّكَانٍۢ بَعِيْدٍ سَمِعُوْا لَهَا تَغَيُّظًا وَّزَفِيْرًا ۝١٣

13. (Moto) utakapowaona katika mahali pa mbali watasikia hasira yake na mngurumo.

وَاِذَآ اُلْقُوْا مِنْهَا مَكَانًا ضَيِّقًا مُّقَرَّنِيْنَ دَعَوْا هُنَالِكَ ثُبُوْرًا ۝١٤ ؕ

14. Na watakapotupwa humo mahali pafinyu hali wamefungwa ndipo hapo wataita angamizo.

لَا تَدْعُوا الْيَوْمَ ثُبُوْرًا وَّاحِدًا وَّادْعُوْا ثُبُوْرًا كَثِيْرًا ۝١٥

15. Msiite leo angamizo moja, bali iteni maangamizo mengi.

قُلْ اَذٰلِكَ خَيْرٌ اَمْ جَنَّةُ الْخُلْدِ الَّتِيْ وُعِدَ الْمُتَّقُوْنَ ۭ كَانَتْ لَهُمْ جَزَاۗءً وَّمَصِيْرًا ۝١٦

16. Sema: Je, haya ni bora au Pepo ya milele ambayo waliahidiwa wachaMungu? Ndiyo kwa ajili yao malipo na marudio·

لَهُمْ فِيْهَا مَا يَشَآءُوْنَ خٰلِدِيْنَ ؕ كَانَ عَلٰى
رَبِّكَ وَعْدًا مَّسْـُٔوْلًا ﴿١٧﴾

17. Watapata humo watakayoyataka; wakaao (humo). Hii ni ahadi iliyo juu ya Mola wako kuitimiza.

وَيَوْمَ يَحْشُرُهُمْ وَمَا يَعْبُدُوْنَ مِنْ دُوْنِ
اللّٰهِ فَيَقُوْلُ ءَاَنْتُمْ اَضْلَلْتُمْ عِبَادِىْ
هٰٓؤُلَآءِ اَمْ هُمْ ضَلُّوا السَّبِيْلَ ﴿١٨﴾

18. Na Siku Atakayowakusanya hawa na wale wanaowaabudu badala ya Allah, basi Atasema: Je, ninyi mmewapoteza watumishi Wangu hawa au wenyewe wamepotea njia?

قَالُوْا سُبْحٰنَكَ مَا كَانَ يَنْۢبَغِىْ لَنَآ اَنْ
نَّتَّخِذَ مِنْ دُوْنِكَ مِنْ اَوْلِيَآءَ وَلٰكِنْ
مَّتَّعْتَهُمْ وَاٰبَآءَهُمْ حَتّٰى نَسُوا الذِّكْرَ ۚ
وَكَانُوْا قَوْمًۢا بُوْرًا ﴿١٩﴾

19. Watasema: Wewe ndiwe Mtakatifu; haikutupasa kushika walinzi badala Yako, lakini Wewe Uliwafaidisha wao na baba zao hata wakasahau mawaidha, na wakawa watu waangamiao.

فَقَدْ كَذَّبُوْكُمْ بِمَا تَقُوْلُوْنَ ۙ فَمَا
تَسْتَطِيْعُوْنَ صَرْفًا وَّلَا نَصْرًا ۚ وَمَنْ
يَّظْلِمْ مِّنْكُمْ نُذِقْهُ عَذَابًا كَبِيْرًا ﴿٢٠﴾

20. Na bila shaka walishawakadhibisheni kwa yale mnayoyasema; na hamtaweza kuondoa (adhabu) wala (kupata) msaada. Na atakayedhulumu miongoni mwenu Tutamwonjesha adhabu kubwa.

وَمَآ اَرْسَلْنَا قَبْلَكَ مِنَ الْمُرْسَلِيْنَ اِلَّآ
اِنَّهُمْ لَيَاْكُلُوْنَ الطَّعَامَ وَيَمْشُوْنَ فِى
الْاَسْوَاقِ ؕ وَجَعَلْنَا بَعْضَكُمْ لِبَعْضٍ
فِتْنَةً ؕ اَتَصْبِرُوْنَ ۚ وَكَانَ رَبُّكَ
بَصِيْرًا ﴿٢٠﴾ ع ٢ ١٧

21. Na Hatukupeleka kabla yako Mitume ila bila shaka walikuwa wakila chakula na wakitembea masokoni; na Tumewajaalia baadhi yenu wawe majaribio kwa wengine; je mtavumilia? Na Mola wako ndiye Aonaye.

JUZU 19

FUNGU 3

وَقَالَ الَّذِيْنَ لَا يَرْجُوْنَ لِقَآءَنَا
لَوْلَآ اُنْزِلَ عَلَيْنَا الْمَلٰٓئِكَةُ اَوْ نَرٰى رَبَّنَا ؕ
لَقَدِ اسْتَكْبَرُوْا فِىْٓ اَنْفُسِهِمْ وَعَتَوْ
عُتُوًّا كَبِيْرًا ﴿٢١﴾

22. Na walisema wale wasiotumai kukutana nasi: Mbona sisi hatuteremshiwi Malaika, au kumwona Mola wetu? Bila shaka wamejitukuza katika nafsi zao na wameasi uasi mkubwa.

Aya 22. Tumekwisha ona mara nyingi kuteremshiwa Malaika na kumwona Allah mradi wake ni kwamba wasioamini walitaka adhabu, kama inavyooneshwa katika Aya ifuatayo. Pia mradi wa Aya hii unaweza kuwa hivi ya kwamba makafiri walitaka nao washukiwe na Malaika kuja ambiwa kuwa wahyi ulioshuka kwa Mtume *s.a.w.* ni haki, na pia wamwone Allah anayewatuma Malaika hao.

يَوْمَ يَرَوْنَ الْمَلٰٓئِكَةَ لَا بُشْرٰى يَوْمَئِذٍ لِّلْمُجْرِمِيْنَ وَ يَقُوْلُوْنَ حِجْرًا مَّحْجُوْرًا ﴿٢٢﴾

23. Siku watakayowaona Malaika haitakuwa furaha siku hiyo kwa wenye makosa; na watasema: Kuwe na kizuizi kizuiacho.

وَقَدِمْنَآ اِلٰى مَا عَمِلُوْا مِنْ عَمَلٍ فَجَعَلْنٰهُ هَبَآءً مَّنْثُوْرًا ﴿٢٣﴾

24. Kisha Tukakigeukia kila kitendo walichofanya miongoni mwa matendo yao na Tukakifanya mavumbi yaliyotapanywa.

اَصْحٰبُ الْجَنَّةِ يَوْمَئِذٍ خَيْرٌ مُّسْتَقَرًّا وَّاَحْسَنُ مَقِيْلًا ﴿٢٤﴾

25. Watu wa Peponi siku hiyo watakuwa katika makao mema na mahali penye starehe njema.

وَ يَوْمَ تَشَقَّقُ السَّمَآءُ بِالْغَمَامِ وَنُزِّلَ الْمَلٰٓئِكَةُ تَنْزِيْلًا ﴿٢٥﴾

26. Na siku itakapopasuka mbingu kwa mawingu, na watateremshwa Malaika kwa wingi.

اَلْمُلْكُ يَوْمَئِذِ ِالْحَقُّ لِلرَّحْمٰنِ ؕ وَكَانَ يَوْمًا عَلَى الْكٰفِرِيْنَ عَسِيْرًا ﴿٢٦﴾

27. Ufalme wa haki siku hiyo utakuwa wa Rahmani, na itakuwa ni siku ngumu kwa makafiri.

وَيَوْمَ يَعَضُّ الظَّالِمُ عَلٰى يَدَيْهِ يَقُوْلُ يٰلَيْتَنِى اتَّخَذْتُ مَعَ الرَّسُوْلِ سَبِيْلًا ﴿٢٧﴾

28. Jihadharini kuhusu siku ambapo mdhalimu atajiuma mikono yake akisema; Laiti ningalishika njia pamoja na Mtume.

يٰوَيْلَتٰى لَيْتَنِىْ لَمْ اَتَّخِذْ فُلَانًا خَلِيْلًا ﴿٢٨﴾

29. Eee Ole wangu! Laiti nisingalimfanya fulani kuwa rafiki.

لَقَدْ اَضَلَّنِىْ عَنِ الذِّكْرِ بَعْدَ اِذْ جَآءَنِىْ ؕ وَكَانَ الشَّيْطٰنُ لِلْاِنْسَانِ خَذُوْلًا ﴿٢٩﴾

30. Kwa yakini yeye alinipoteza katika mawaidha baada ya kunifikia; na Shetani ndiye amtupaye mwanadamu.

وَقَالَ الرَّسُوْلُ يٰرَبِّ اِنَّ قَوْمِى اتَّخَذُوْا هٰذَا الْقُرْاٰنَ مَهْجُوْرًا ﴿٣٠﴾

31. Na Mtume atasema: Ee Mola wangu, hakika watu wangu wameifanya Qur'an hii kuwa kitu kilichoachwa.

Aya 26. Bishara hii kama tulivyokwisha eleza, ilitimia siku ya vita vya Badri. Siku ile Waislamu walikuwa upande wa tifutifu la mchanga, na makafiri upande wenye ardhi ngumu. Mvua ilipiga na mchanga ukakamatana ukawa mgumu, na upande wa makafiri ukawa na tope na utelezi. Malaika wa Allah walishuka kuwasaidia Waislamu, na makafiri wakashindwa sana katika vita hiyo.

Aya 29. Wangapi wamelia na watalia kilio kama hiki: Marafiki wabaya huwapoteza rafiki zao, na marafiki wema huongoza. Kwa sababu hii Mtume *s.a.w* ametufunza kuomba, "Mola wangu unirahisishie kupata rafiki mwema," na Allah amesema "Kuweni pamoja na wasemao kweli" (sura 9:119). Kwa kuepuka marafiki wabaya mtu anapona katika hatari nyingi.

Aya 31. *Qaala.* Neno hili liko katika hali ya tamko lililosemwa wakati uliopita, yaani

وَكَذٰلِكَ جَعَلْنَا لِكُلِّ نَبِيٍّ عَدُوًّا مِّنَ الْمُجْرِمِيْنَ ؕ وَكَفٰى بِرَبِّكَ هَادِيًا وَّنَصِيْرًا ﴿٣١﴾

32. Na vivi hivi Tumemfanyia kila Nabii adui miongoni mwa wakosefu; na Mola wako Anatosha kuwa Kiongozi na Msaidizi.

وَقَالَ الَّذِيْنَ كَفَرُوْا لَوْلَا نُزِّلَ عَلَيْهِ الْقُرْاٰنُ جُمْلَةً وَّاحِدَةً ۚ كَذٰلِكَ ۚ لِنُثَبِّتَ بِهٖ فُؤَادَكَ وَرَتَّلْنٰهُ تَرْتِيْلًا ﴿٣٢﴾

33. Na wakasema wale walioku-furu: Mbona haikuteremshwa kwake Qur'an yote mara moja? Kama hivyo, ili Tukuimarishe kwayo moyo wako, na Tumeipanga kwa mpango.

وَلَا يَاْتُوْنَكَ بِمَثَلٍ اِلَّا جِئْنٰكَ بِالْحَقِّ وَاَحْسَنَ تَفْسِيْرًا ﴿٣٣﴾

34. Wala hawatakuletea mfano wo wote, bali Sisi Tunakuletea yaliyo haki na tafsiri iliyo bora.

اَلَّذِيْنَ يُحْشَرُوْنَ عَلٰى وُجُوْهِهِمْ اِلٰى جَهَنَّمَ ۙ اُولٰٓئِكَ شَرٌّ مَّكَانًا وَّاَضَلُّ سَبِيْلًا ﴿٣٤﴾ ع ٤

35. (Ama) wale watakaokusanywa kifudifudi kwenye Jahanamu, hao watakuwa mahali pabaya na ndio wenye kuipotea sana njia.

FUNGU 4

وَلَقَدْ اٰتَيْنَا مُوْسَى الْكِتٰبَ وَجَعَلْنَا مَعَهٗۤ اَخَاهُ هٰرُوْنَ وَزِيْرًا ﴿٣٥﴾ ۚ

36. Bila shaka Tulimpa Musa Kitabu na Tukamweka pamoja naye nduguye Harun kuwa waziri.

فَقُلْنَا اذْهَبَاۤ اِلَى الْقَوْمِ الَّذِيْنَ كَذَّبُوْا بِاٰيٰتِنَا ؕ فَدَمَّرْنٰهُمْ تَدْمِيْرًا ﴿٣٦﴾

37. Tukawaambia: Nendeni kwa watu waliokadhibisha Aya Zetu; basi Tukawaangamiza kabisa.

---

alisema. Hapa tumelifasiri *atasema* ili kufuata kanuni ya matamko ya bishara za Qur'an. Inapokuwa inabashiria jambo ambalo kwa yakini litatokea inasema kwa namna kana kwamba jambo hilo limekwisha tokea, maana mbele ya Allah jambo analojua litatokea ni sawa kabisa na lile lililokwisha tokea, kwani hakuna kinyume ila litatokea tu.

Wameifanya Qur'an kuwa kitu kilichoachwa. Maneno haya ni bishara inayoelezwa kwa namna ya masikitiko ya Mtume *s.a.w.* ya kuwa maanguko ya umati wake ni kwa sababu wameiacha Qur'an. Kwa kweli ni jambo la kusikitisha kuona watu hawajali kutaka kujua Qur'an inaagiza nini ili wafuate na wapate kutukuka. Wao hungoja mtu afe, ndipo hutandika majamvi na kumsomea hitima. Je aliyekufa itamfaa nini Qur'an akiisomewa? Mtu asome Qur'an au asomeshwe angali mzima na afuate maagizo yake ndipo itamfaa.

Aya 33. *Na Tumeipanga kwa mpango.* Maneno haya yanakanusha usemi wa watu wasemao ya kuwa Qur'an ilikuwa imetawanyika bila mpango wo wote na Seyidna Abu Bakar au Seyidna Uthman ndiye aliyeipanga. Aya hii inaonyesha ya kuwa Mtume *s.a.w.* mwenyewe aliweka mpango ule ule uliotakiwa na Allah (Tazama sura 75:17-20).

وَقَوْمَ نُوْحٍ لَّمَّا كَذَّبُوا الرُّسُلَ اَغْرَقْنٰهُمْ
وَجَعَلْنٰهُمْ لِلنَّاسِ اٰيَةً ؕ وَاَعْتَدْنَا لِلظّٰلِمِيْنَ
عَذَابًا اَلِيْمًا ﴿۳۸﴾

38. Na watu wa Nuhu, walipowakadhibisha Mitume Tukawagharikisha na Tukawafanya Ishara kwa ajili ya wanadamu; na Tukawaandalia wadhalimu adhabu iumizayo.

وَّ عَادًا وَّ ثَمُوْدَا۠ وَاَصْحٰبَ الرَّسِّ
وَقُرُوْنًۢا بَيْنَ ذٰلِكَ كَثِيْرًا ﴿۳۹﴾

39. Na Waadi na Wathamudi na watu wa Rass na vizazi vingi vilivyokuwa kati yao.

وَكُلًّا ضَرَبْنَا لَهُ الْاَمْثَالَ ۫ وَكُلًّا
تَبَّرْنَا تَتْبِيْرًا ﴿۴۰﴾

40. Na wote tuliwapigia mifano ya watu wa zamani; na wote Tuliwaangamiza kabisa.

وَلَقَدْ اَتَوْا عَلَى الْقَرْيَةِ الَّتِيْۤ اُمْطِرَتْ
مَطَرَ السَّوْءِ ؕ اَفَلَمْ يَكُوْنُوْا يَرَوْنَهَا ۚ
بَلْ كَانُوْا لَا يَرْجُوْنَ نُشُوْرًا ﴿۴۱﴾

41. Na kwa yakini wao walifika kwenye mji ulionyeshewa mvua mbaya, basi je hawakuwa wakiuona, bali walikuwa hatarajii kufufuliwa.

وَ اِذَا رَاَوْكَ اِنْ يَّتَّخِذُوْنَكَ اِلَّا هُزُوًا ؕ
اَهٰذَا الَّذِىْ بَعَثَ اللّٰهُ رَسُوْلًا ﴿۴۲﴾

42. Na wanapokuona hawakufanyii ila mzaha tu: Je, huyu ndiye Allah Aliyemtuma kuwa Mtume?

اِنْ كَادَ لَيُضِلُّنَا عَنْ اٰلِهَتِنَا لَوْلَاۤ اَنْ صَبَرْنَا
عَلَيْهَا ؕ وَسَوْفَ يَعْلَمُوْنَ حِيْنَ يَرَوْنَ
الْعَذَابَ مَنْ اَضَلُّ سَبِيْلًا ﴿۴۳﴾

43. Kwa hakika alikuwa karibu kutupoteza kwa miungu yetu, kama tusingalidumu juu yao. Na karibu watajua, watakapoiona adhabu, ni nani aliyepotea njia.

اَرَءَيْتَ مَنِ اتَّخَذَ اِلٰهَهٗ هَوٰىهُ ؕ اَفَاَنْتَ
تَكُوْنُ عَلَيْهِ وَكِيْلًا ﴿۴۴﴾

44. Je, ulimwona yule aliyefanya tamanio lake kuwa mungu wake? Basi je, utakuwa mdhamini wake?

اَمْ تَحْسَبُ اَنَّ اَكْثَرَهُمْ يَسْمَعُوْنَ اَوْ
يَعْقِلُوْنَ ؕ اِنْ هُمْ اِلَّا كَالْاَنْعَامِ ۚ بَلْ
هُمْ اَضَلُّ سَبِيْلًا ﴿۴۴﴾ ع

45. Au je, unafikiri ya kwamba wengi wao wanasikia au wanafahamu? Hao sio ila ni kama wanyama, bali wao wameipotea zaidi njia.

Aya 39. *Watu wa Rass.* Zajjaj anaeleza ya kuwa Rass ni mahali walipokaa baadhi ya watu wa kabila la Thamud; na wengine wanasema Rass ni jina la mji katika Yamama (Taj). Kadhalika neno rass pia lina maana ya *kisima* na inafikiriwa ya kuwa *watu wa kisima* ni nduguze Nabii Yusuf waliomtupa kisimani; nayo hii ndio rai ya mwanachuoni mkubwa, Hadhrat Nur-ud-Din, Khalifa wa Kwanza wa Masihi Aliyeahidiwa.

Aya 41. Mji uliotajwa katika Aya hii ni ule wa Sodom ulio katika njia kuu ya kwenda Sham ambao uliadhibiwa na Allah.

FUNGU 5

46. Je, hukuona Mola wako jinsi Alivyokitandaza kivuli? Na Angalitaka bila shaka Angekifanya kitulie; kisha Tumelifanya jua liwe dalili juu yake.

47. Kisha Tunakivutia Kwetu kidogo kidogo.

48. Naye ndiye Aliyewafanyieni usiku kuwa kivazi na usingizi kuwa maburudisho, na Akaufanya mchana uwe kwa kutawanyika.

49. Naye ndiye Azitumaye pepo kuwa habari njema kabla ya (kufika) rehema Yake; na Tunayateremsha kutoka mawinguni maji safi;

50. Ili kwayo Tuihuishe nchi iliyokufa na Tuwanyweshe hayo baadhi ya Tuliowaumba katika wanyama na watu wengi.

51. Na kwa yakini Tumeieleza baina yao mara kwa mara ili wakumbuke; lakini watu wengi wakakataa ila kukufuru tu.

52. Na kama Tungetaka Tungewapelekea katika kila mji, Mwonyaji.

53. Basi usiwatii makafiri na ushindane nao kwa (Qur'an) hii mashindano makubwa.

54. Naye ndiye Aliyeziunganisha bahari mbili, hii ni tamu, itulizayo kiu, na hii ni yenye chumvi kali; na Akaweka kinga kati yao na kizuizi kizuiacho.

اَلَمْ تَرَ اِلٰى رَبِّكَ كَيْفَ مَدَّ الظِّلَّ ۚ وَلَوْ
شَآءَ لَجَعَلَهٗ سَاكِنًا ۚ ثُمَّ جَعَلْنَا الشَّمْسَ
عَلَيْهِ دَلِيْلًا ۙ﴿٤٦﴾
ثُمَّ قَبَضْنٰهُ اِلَيْنَا قَبْضًا يَّسِيْرًا ﴿٤٧﴾
وَهُوَ الَّذِىْ جَعَلَ لَكُمُ الَّيْلَ لِبَاسًا وَّالنَّوْمَ
سُبَاتًا وَّجَعَلَ النَّهَارَ نُشُوْرًا ﴿٤٨﴾
وَهُوَ الَّذِىْٓ اَرْسَلَ الرِّيٰحَ بُشْرًا ۢ بَيْنَ يَدَىْ
رَحْمَتِهٖ ۚ وَاَنْزَلْنَا مِنَ السَّمَآءِ مَآءً طَهُوْرًا ۙ﴿٤٩﴾
لِّنُحْيِىَ بِهٖ بَلْدَةً مَّيْتًا وَّنُسْقِيَهٗ مِمَّا
خَلَقْنَآ اَنْعَامًا وَّاَنَاسِىَّ كَثِيْرًا ﴿٥٠﴾
وَلَقَدْ صَرَّفْنٰهُ بَيْنَهُمْ لِيَذَّكَّرُوْا ۖ فَاَبٰٓى
اَكْثَرُ النَّاسِ اِلَّا كُفُوْرًا ﴿٥١﴾
وَلَوْ شِئْنَا لَبَعَثْنَا فِىْ كُلِّ قَرْيَةٍ نَّذِيْرًا ﴿٥٢﴾
فَلَا تُطِعِ الْكٰفِرِيْنَ وَجَاهِدْهُمْ بِهٖ
جِهَادًا كَبِيْرًا ﴿٥٣﴾
وَهُوَ الَّذِىْ مَرَجَ الْبَحْرَيْنِ هٰذَا عَذْبٌ
فُرَاتٌ وَّهٰذَا مِلْحٌ اُجَاجٌ ۚ وَجَعَلَ بَيْنَهُمَا
بَرْزَخًا وَّحِجْرًا مَّحْجُوْرًا ﴿٥٤﴾

Aya 53. *Jihaadan kabiiran* "Jihadi kubwa." Aya hii inaeleza kuwa Jihadi au mashindano makubwa hutakiwa yaendeshwe kwa kuihubiri Qur'an; siyo kushika upanga tu. Hivyo wanaodhani ya kuwa jihadi ni kushika upanga na kuwasilimisha makafiri kwa nguvu wanakosea sana. Waislamu hufanya Jihadi ya upanga pale maadui zao wanapoleta panga ili kuwachinja na kuwashurutisha kuacha dini yao. Hapo Waislamu huchaga na panga wakijitetea. Lakini jihadi kubwa ya dini ya Kiislamu ni kuwasuluhisha watu kwa Qur'an. Pia imeelezwa katika Hadithi ya kuwa Jihadi kubwa zaidi ni mtu kufanya bidii kuushinda moyo wake. (Tirmidh).

55. Naye ndiye Aliyemwumba mwanadamu kwa maji, kisha Akamfanyia nasabu na ujamaa wa ndoa. Na Mola wako ni Mwenye uwezo.

وَهُوَ الَّذِیْ خَلَقَ مِنَ الْمَآءِ بَشَرًا فَجَعَلَهٗ نَسَبًا وَّ صِهْرًا ؕ وَ كَانَ رَبُّكَ قَدِیْرًا ﴿۵۴﴾

56. Na wanayaabudu kinyume cha Allah yasiyowafaa wala yasiyowadhuru; na kafiri ni msaidizi dhidi ya Mola wake.

وَ یَعْبُدُوْنَ مِنْ دُوْنِ اللّٰهِ مَا لَا یَنْفَعُهُمْ وَ لَا یَضُرُّهُمْ ؕ وَ كَانَ الْكَافِرُ عَلٰی رَبِّهٖ ظَهِیْرًا ﴿۵۵﴾

57. Nasi Hatukukutuma ila uwe Mtoaji wa habari njema na Mwonyaji.

وَ مَاۤ اَرْسَلْنٰكَ اِلَّا مُبَشِّرًا وَّ نَذِیْرًا ﴿۵۶﴾

58. Sema: Siwaombeni ujira juu yake, isipokuwa mwenye kutaka ashike njia iendayo kwa Mola wake.

قُلْ مَاۤ اَسْـَٔلُكُمْ عَلَیْهِ مِنْ اَجْرٍ اِلَّا مَنْ شَآءَ اَنْ یَّتَّخِذَ اِلٰی رَبِّهٖ سَبِیْلًا ﴿۵۷﴾

59. Na umtegemee mzima wa milele Ambaye Hatakufa, na umtukuze kwa sifa Zake njema. Naye Anatosha kwa dhambi za watumishi Wake kuwa Mwenye habari nazo.

وَ تَوَكَّلْ عَلَی الْحَیِّ الَّذِیْ لَا یَمُوْتُ وَ سَبِّحْ بِحَمْدِهٖ ؕ وَ كَفٰی بِهٖ بِذُنُوْبِ عِبَادِهٖ خَبِیْرَ ۨ ﴿۵۸﴾

60. Ambaye Aliziumba mbingu na ardhi na vilivyomo kati yao katika nyakati sita, kisha Akastawi juu ya Arshi; Mwingi wa Huruma, tafuta habari kutoka Kwake ukiamaini kwamba Yeye Ndiye Mjuzi wa habari.

الَّذِیْ خَلَقَ السَّمٰوٰتِ وَ الْاَرْضَ وَ مَا بَیْنَهُمَا فِیْ سِتَّةِ اَیَّامٍ ثُمَّ اسْتَوٰی عَلَی الْعَرْشِ ۛؕ اَلرَّحْمٰنُ فَسْـَٔلْ بِهٖ خَبِیْرًا ﴿۵۹﴾

61. Na wanapoambiwa, Msujudieni Rahman, husema: Ni nani Rahmani? Je tumsujudie unayetuamuru? Na inawazidishia chuki.

وَ اِذَا قِیْلَ لَهُمُ اسْجُدُوْا لِلرَّحْمٰنِ قَالُوْا وَ مَا الرَّحْمٰنُ ۗ اَنَسْجُدُ لِمَا تَاْمُرُنَا وَ زَادَهُمْ نُفُوْرًا ﴿۶۰﴾ ۩

FUNGU 6

62. Mwenye mibaraka ni Yule Ambaye Amejaalia vituo vya nyota mbinguni na Akajaalia humo jua ling'aalo na mwezi ung'aao.

تَبٰرَكَ الَّذِیْ جَعَلَ فِی السَّمَآءِ بُرُوْجًا وَّ جَعَلَ فِیْهَا سِرٰجًا وَّ قَمَرًا مُّنِیْرًا ﴿۶۱﴾

63. Naye ndiye Aliyefanya usiku na mchana vifuatane kwa yule anayetaka kushika nasaha au anayetaka kushukuru.

وَ هُوَ الَّذِیْ جَعَلَ الَّیْلَ وَ النَّهَارَ خِلْفَةً لِّمَنْ اَرَادَ اَنْ یَّذَّكَّرَ اَوْ اَرَادَ شُكُوْرًا ﴿۶۲﴾

وَعِبَادُ الرَّحْمٰنِ الَّذِيْنَ يَمْشُوْنَ عَلَى الْاَرْضِ هَوْنًا وَّ اِذَا خَاطَبَهُمُ الْجٰهِلُوْنَ قَالُوْا سَلٰمًا ﴿٦٣﴾

64. Na watumishi wa Rahmani ni wale wanaotembea ardhini kwa unyenyekevu, na wajinga wakisema nao husema: Amani;

وَالَّذِيْنَ يَبِيْتُوْنَ لِرَبِّهِمْ سُجَّدًا وَّ قِيَامًا ﴿٦٤﴾

65. Na wale wanaokesha usiku kwa ajili ya Mola wao kwa kusujudu na kusimama:

وَالَّذِيْنَ يَقُوْلُوْنَ رَبَّنَا اصْرِفْ عَنَّا عَذَابَ جَهَنَّمَ ۖ اِنَّ عَذَابَهَا كَانَ غَرَامًا ﴿٦٥﴾

66. Na wale wanaosema: Mola wetu, Utuondolee adhabu ya Jahanamu, bila shaka adhabu yake ndiyo iendeleayo.

اِنَّهَا سَآءَتْ مُسْتَقَرًّا وَّ مُقَامًا ﴿٦٦﴾

67. Hakika (Jahanamu) hiyo ni kituo kibaya na mahali (pabaya) pa kukaa.

وَالَّذِيْنَ اِذَآ اَنْفَقُوْا لَمْ يُسْرِفُوْا وَلَمْ يَقْتُرُوْا وَكَانَ بَيْنَ ذٰلِكَ قَوَامًا ﴿٦٧﴾

68. Na wale ambao wanapotumia hawatumii kwa fujo wala hawafanyi ubahili, na wanakuwa waadilifu baina ya hayo.

وَالَّذِيْنَ لَا يَدْعُوْنَ مَعَ اللّٰهِ اِلٰهًا اٰخَرَ وَلَا يَقْتُلُوْنَ النَّفْسَ الَّتِيْ حَرَّمَ اللّٰهُ اِلَّا بِالْحَقِّ وَلَا يَزْنُوْنَ ۚ وَمَنْ يَّفْعَلْ ذٰلِكَ يَلْقَ اَثَامًا ﴿٦٨﴾

69. Na wale wasiomwomba mungu mwingine pamoja na Allah, wala hawaui nafsi aliyoiharimisha Allah isipokuwa kwa haki, wala hawazini, na atakayefanya hilo bila shaka atakutana na (adhabu ya) dhambi.

يُّضٰعَفْ لَهُ الْعَذَابُ يَوْمَ الْقِيٰمَةِ وَ يَخْلُدْ فِيْهٖ مُهَانًا ﴿٦٩﴾

70. Atazidishiwa adhabu siku ya Kiyama, na atakaa humo kwa kufedheheka.

اِلَّا مَنْ تَابَ وَاٰمَنَ وَعَمِلَ عَمَلًا صَالِحًا فَاُولٰٓئِكَ يُبَدِّلُ اللّٰهُ سَيِّاٰتِهِمْ حَسَنٰتٍ ؕ وَكَانَ اللّٰهُ غَفُوْرًا رَّحِيْمًا ﴿٧٠﴾

71. Ila yule aliyetubia na kuamini na kufanya vitendo vizuri; basi hao ndio Allah Atawabadilishia maovu yao kuwa mema; na Allah ni Msamehevu, Mrehemevu.

وَمَنْ تَابَ وَعَمِلَ صَالِحًا فَاِنَّهٗ يَتُوْبُ اِلَى اللّٰهِ مَتَابًا ﴿٧١﴾

72. Na aliyetubia na kufanya wema, basi kwa hakika yeye anatubu kwa Allah toba hasa.

Aya 64. Aya hii na zingine zifuatazo zinaonyesha mwujiza mkubwa wa Mtume *s.a.w.* namna alivyowabadilisha watu waliokuwa na kila namna ya ubaya wakawa wenye sifa bora za ucha-Mungu zinazotajwa hapo. Hii ndiyo kazi ya ajabu iliyofanywa na Mtume *s.a.w.* ambayo haina mfano katika historia ya dunia.

73. Na wale ambao hawashuhudii uwongo, na wanapopita penye upuuzi, hupita kwa heshima.

وَالَّذِيْنَ لَا يَشْهَدُوْنَ الزُّوْرَ ۙ وَ اِذَا مَرُّوْا بِاللَّغْوِ مَرُّوْا كِرَامًا ﴿٧٢﴾

74. Na wale ambao wanapokumbushwa Aya za Mola wao hawaziangukii kwa uziwi na upofu.

وَالَّذِيْنَ اِذَا ذُكِّرُوْا بِاٰيٰتِ رَبِّهِمْ لَمْ يَخِرُّوْا عَلَيْهَا صُمًّا وَّ عُمْيَانًا ﴿٧٣﴾

75. Na wale wanaosema: Mola wetu! Utupe katika wake zetu na watoto wetu yaburudishayo macho, na Utujaalie kuwa viongozi kwa wamchao (Mungu).

وَالَّذِيْنَ يَقُوْلُوْنَ رَبَّنَا هَبْ لَنَا مِنْ اَزْوَاجِنَا وَذُرِّيّٰتِنَا قُرَّةَ اَعْيُنٍ وَّ اجْعَلْنَا لِلْمُتَّقِيْنَ اِمَامًا ﴿٧٤﴾

76. Hao ndio watakaolipwa ghorofa kwa kuwa walisubiri, na watapokelewa humo kwa maamkio na amani;

اُولٰٓئِكَ يُجْزَوْنَ الْغُرْفَةَ بِمَا صَبَرُوْا وَيُلَقَّوْنَ فِيْهَا تَحِيَّةً وَّ سَلٰمًا ﴿٧٥﴾

77. Wakikaa humo: kituo kizuri na mahali pazuri pa kukaa.

خٰلِدِيْنَ فِيْهَا ؕ حَسُنَتْ مُسْتَقَرًّا وَّ مُقَامًا ﴿٧٦﴾

78. Sema: Mola wangu hangewajalini kama si kuomba kwenu; ninyi mmekwisha kadhibisha, kwa hiyo hivi karibuni (adhabu) itakuwa yenye kushika.

قُلْ مَا يَعْبَؤُا بِكُمْ رَبِّيْ لَوْلَا دُعَآؤُكُمْ ۚ فَقَدْ كَذَّبْتُمْ فَسَوْفَ يَكُوْنُ لِزَامًا ﴿٧٧﴾ ع

Aya 74. Aya hii inaonyesha ya kuwa dini ya Kiislamu haitaki watu wafuate mambo, hata kama ni ya dini, kama viziwi na vipofu, bali washike kila jambo kwa busara na akili.

سُوْرَةُ الشُّعَرَآءِ مَكِّيَّةٌ وَّ هِيَ مَعَ الْبَسْمَلَةِ مِائَتَانِ وَثَمَانٍ وَّ عِشْرُوْنَ اٰيَةً وَّ اَحَدَ عَشَرَ رُكُوْعًا

26. SURA ASH-SHU'ARAA

Imeteremshwa Makka

Ina mafungu 11 na Aya 228 pamoja na Bismillahi

بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ ①

1. Kwa jina la Allah, Mwingi wa rehema, Mwingi wa ukarimu.

طٰسٓمّٓ ②

2. (Allah) Atakasaye, Asikiaye, Ajuaye.

تِلْكَ اٰيٰتُ الْكِتٰبِ الْمُبِيْنِ ③

3. Hizi ni Aya za Kitabu kielezacho.

لَعَلَّكَ بَاخِعٌ نَّفْسَكَ اَلَّا يَكُوْنُوْا مُؤْمِنِيْنَ ④

4. Huenda utaangamiza nafsi yako kwa sababu hawawi waaminio.

اِنْ نَّشَاْ نُنَزِّلْ عَلَيْهِمْ مِّنَ السَّمَآءِ اٰيَةً فَظَلَّتْ اَعْنَاقُهُمْ لَهَا خٰضِعِيْنَ ⑤

5. Tungependa Tungewateremshia kutoka mbinguni Ishara na shingo zao ziwe zenye kuinamia.

وَمَا يَاْتِيْهِمْ مِّنْ ذِكْرٍ مِّنَ الرَّحْمٰنِ مُحْدَثٍ اِلَّا كَانُوْا عَنْهُ مُعْرِضِيْنَ ⑥

6. Wala hauwafikii ukumbusho mpya utokao kwa Rahmani ila hujitenga mbali nao.

فَقَدْ كَذَّبُوْا فَسَيَاْتِيْهِمْ اَنْۢبٰٓؤُا مَا كَانُوْا بِهٖ يَسْتَهْزِءُوْنَ ⑦

7. Basi kwa yakini wamekadhibisha, kwa hiyo karibuni zitawafikia habari za yale waliyokuwa wakiyafanyia mzaha.

Jina la sura hii limetolewa katika Aya 225 inayotaka kueleza ya kuwa hii Qur'an si kazi ya mtunga mashairi maana haifanani na kazi ya watungao mashairi. Mara kwa mara mashtaka yaliyoletwa juu ya Qur'an ni kwamba ilikuwa mashairi yaliyotungwa na Mtume *s.a.w.* na Qur'an ikabatilisha mashtaka hayo na kuonyesha ya kuwa kazi ya Mtume *s.a.w.* ilikuwa sawa na kazi ya Manabii waliomtangulia. Sura hii ilishuka Makka.

Aya 2. *Taa Siin Miim. Taa* ni *Taahir* (Atakasaye), *Siin* ni *Samii'* (Asikiaye), na *Miim* ni *'Aliim* (Ajuaye). Hizo ndizo sifa za Allah zinazoelezwa na herufi hizo za mkato.

Aya 4. Aya hii inaonyesha namna Mtume *s.a.w.* alivyokuwa na huruma na masikitiko juu ya hali ya watu kukosa kuamini, akafanya kila namna ya juhudi ili watu wapate kuongoka, na kila wakati hufikiri kutoamini kwao na hupata majonzi sana.

Aya 6. *Ukumbusho mpya*, yaani mauidha yanayofika kwa namna mpya.

8. Je, hawakuiona ardhi, mimea mingapi Tumeimeesha humo ya kila namna nzuri?

اَوَلَمۡ يَرَوۡا اِلَى الۡاَرۡضِ كَمۡ اَنۡۢبَتۡنَا فِيۡهَا مِنۡ كُلِّ زَوۡجٍ كَرِيۡمٍ ۝٨

9. Bila shaka katika hayo imo Ishara, lakini wengi wao si waaminio.

اِنَّ فِىۡ ذٰلِكَ لَاٰيَةً ؕ وَمَا كَانَ اَكۡثَرُهُمۡ مُّؤۡمِنِيۡنَ ۝٩

10. Na hakika Mola wako Yeye ndiye Mwenye nguvu, Mwenye rehema.

وَاِنَّ رَبَّكَ لَهُوَ الۡعَزِيۡزُ الرَّحِيۡمُ ۝١٠ ع

FUNGU 2

11. Na Mola wako Alipomwita Musa, ya kwamba: ufike kwa watu wadhalimu.

وَاِذۡ نَادٰى رَبُّكَ مُوۡسٰۤى اَنِ ائۡتِ الۡقَوۡمَ الظّٰلِمِيۡنَ ۙ ۝١١

12. Watu wa Firauni; je, hawaogopi?

قَوۡمَ فِرۡعَوۡنَ ؕ اَلَا يَتَّقُوۡنَ ۝١٢

13. Akasema Mola wangu hakika mimi naogopa kuwa watanikadhibisha.

قَالَ رَبِّ اِنِّىۡۤ اَخَافُ اَنۡ يُّكَذِّبُوۡنِ ۫ ۝١٣

14. Na kifua changu kinadhikika na ulimi wangu hautamki vema, basi (pia) Upeleke (ujumbe) kwa Harun.

وَيَضِيۡقُ صَدۡرِىۡ وَلَا يَنۡطَلِقُ لِسَانِىۡ فَاَرۡسِلۡ اِلٰى هٰرُوۡنَ ۝١٤

15. Nao wanalo kosa kwangu, hivyo naogopa wataniua.

وَلَهُمۡ عَلَىَّ ذَنۡۢبٌ فَاَخَافُ اَنۡ يَّقۡتُلُوۡنِ ۚ ۝١٥

16. Akasema: Siyo, basi nendeni na Ishara Zangu; hakika Sisi Tu pamoja nanyi Tunasikia.

قَالَ كَلَّا ۚ فَاذۡهَبَا بِاٰيٰتِنَاۤ اِنَّا مَعَكُمۡ مُّسۡتَمِعُوۡنَ ۝١٦

17. Basi mfikieni Firauni na mwambieni: Bila shaka sisi ni Mitume wa Mola wa walimwengu.

فَاۡتِيَا فِرۡعَوۡنَ فَقُوۡلَاۤ اِنَّا رَسُوۡلُ رَبِّ الۡعٰلَمِيۡنَ ۙ ۝١٧

18. (Tumetumwa) ya kwamba uwapeleke pamoja nasi wana wa Israeli.

اَنۡ اَرۡسِلۡ مَعَنَا بَنِىۡۤ اِسۡرَآءِيۡلَ ؕ ۝١٨

Aya 13. *Mimi naogopa.* Aya hii inaonyesha ya kuwa Nabii Musa hakuwa na tamaa ya kwamba apewe kazi ya unabii; angekuwa radhi kukaa faraghani na kumwabudu Mola wake. Lakini afanyeje na hali Mungu anamwamrisha kutenda kazi hiyo. Hivi ndivyo huwa hali ya Manabii wote, huwa wanajua watu hawatakubali maneno yao, na itawafikia taabu. Kwa kweli kazi ya Manabii ni ya taabu sana, hata mtu mwema asingependa kubebeshwa mzigo wa namna hiyo kwa hiyari yake; lakini kwa kuwa Mungu anataka wafanye basi ndiyo wanafanya.

Aya 15. Ndiyo kusema. Ee Mola wangu ingawa sina kosa Kwako, lakini wao wananiona kama nimewakosea, basi huenda wataniua.

قَالَ اَلَمْ نُرَبِّكَ فِيْنَا وَلِيْدًا وَّ لَبِثْتَ فِيْنَا مِنْ عُمُرِكَ سِنِيْنَ ﴿۱۹﴾

19. (Firauni) akasema: Je, hatukukulea kati yetu (ulipokuwa) mtoto, na ukakaa kati yetu miaka (mingi) ya umri wako?

وَفَعَلْتَ فَعْلَتَكَ الَّتِيْ فَعَلْتَ وَاَنْتَ مِنَ الْكٰفِرِيْنَ ﴿۲۰﴾

20. Na ulifanya kitendo chako kile ulichofanya na ukawa miongoni mwa wasioshukuru.

قَالَ فَعَلْتُهَاۤ اِذًا وَّ اَنَا مِنَ الضَّآلِّيْنَ ﴿۲۱﴾

21. (Musa) akasema: Nilifanya hapo nilipokuwa miongoni mwa wale wasioelewa.

فَفَرَرْتُ مِنْكُمْ لَمَّا خِفْتُكُمْ فَوَهَبَ لِيْ رَبِّيْ حُكْمًا وَّ جَعَلَنِيْ مِنَ الْمُرْسَلِيْنَ ﴿۲۲﴾

22. Basi niliwakimbieni nilipowaogopeni, kisha Mola wangu Akanipa mamlaka na Akanifanya niwe miongoni mwa Mitume.

وَ تِلْكَ نِعْمَةٌ تَمُنُّهَا عَلَيَّ اَنْ عَبَّدْتَّ بَنِيْۤ اِسْرَآءِيْلَ ﴿۲۳﴾

23. Je hiyo ndiyo neema uliyonifanyia ihsani ya kuwatia utumwani wana wa Israeli?

قَالَ فِرْعَوْنُ وَ مَا رَبُّ الْعٰلَمِيْنَ ﴿۲۴﴾

24. Firauni akasema: Na nani Mola wa walimwengu?

قَالَ رَبُّ السَّمٰوٰتِ وَالْاَرْضِ وَمَا بَيْنَهُمَا ؕ اِنْ كُنْتُمْ مُّوْقِنِيْنَ ﴿۲۵﴾

25. (Musa) akasema: Mwumba wa mbingu na ardhi na vilivyomo kati yao, ikiwa ninyi ni wenye yakini.

قَالَ لِمَنْ حَوْلَهٗۤ اَلَا تَسْتَمِعُوْنَ ﴿۲۶﴾

26. (Firauni) akawaambia waliomzunguka: Je, hamsikii?

قَالَ رَبُّكُمْ وَرَبُّ اٰبَآئِكُمُ الْاَوَّلِيْنَ ﴿۲۷﴾

27. (Musa) akasema: Mola wenu na Mola wa baba zenu wa kwanza.

قَالَ اِنَّ رَسُوْلَكُمُ الَّذِيْۤ اُرْسِلَ اِلَيْكُمْ لَمَجْنُوْنٌ ﴿۲۸﴾

28. (Firauni) akasema: Bila shaka Mtume wenu aliyetumwa kwenu ni majnuni.

قَالَ رَبُّ الْمَشْرِقِ وَالْمَغْرِبِ وَمَا بَيْنَهُمَا ؕ اِنْ كُنْتُمْ تَعْقِلُوْنَ ﴿۲۹﴾

29. (Musa) akasema: (Yeye ni) Mola wa mashariki na magharibi na vilivyomo kati yao, ikiwa mnafahamu.

قَالَ لَئِنِ اتَّخَذْتَ اِلٰهًا غَيْرِيْ لَاَجْعَلَنَّكَ مِنَ الْمَسْجُوْنِيْنَ ﴿۳۰﴾

30. (Firauni) akasema: Kama ukishika Mungu mwingine badala yangu, kwa yakini nitakufanya uwe miongoni mwa wafungwa.

Aya 21. Nabii Musa aliwapenda sana watu wake hata hakuelewa afanye nini kumsaidia mtu yule. Hakuwa na nia ya kumwua yule adui, alimpiga kwa konde tu likawa sababu ya ajali yake, kwani kwa desturi mtu hafi kwa konde.

قَالَ اَوَلَوْ جِئْتُكَ بِشَیْءٍ مُّبِیْنٍ ﴿۳۱﴾

31. Akasema: Je, ijapokuwa nikikuletea kitu kilicho wazi?

قَالَ فَاْتِ بِهٖۤ اِنْ كُنْتَ مِنَ الصّٰدِقِیْنَ ﴿۳۲﴾

32. Akasema: Kilete, ikiwa u miongoni mwa wasemao kweli.

فَاَلْقٰی عَصَاهُ فَاِذَا هِیَ ثُعْبَانٌ مُّبِیْنٌ ﴿۳۳﴾

33. Basi akaitupa fimbo yake mara ikawa nyoka dhahiri.

وَّنَزَعَ یَدَهٗ فَاِذَا هِیَ بَیْضَآءُ لِلنّٰظِرِیْنَ ﴿۳۴﴾ ع ۴

34. Na akatoa mkono wake, na mara ukawa mweupe kwa watazamao.

FUNGU 3

قَالَ لِلْمَلَاِ حَوْلَهٗۤ اِنَّ هٰذَا لَسٰحِرٌ عَلِیْمٌ ﴿۳۵﴾ۙ

35. (Firauni) akasema kuwaambia wakuu waliomzunguka: Kwa yakini huyu ni mchawi ajuaye sana:

یُّرِیْدُ اَنْ یُّخْرِجَكُمْ مِّنْ اَرْضِكُمْ بِسِحْرِهٖ ۖ فَمَاذَا تَاْمُرُوْنَ ﴿۳۶﴾

36. Anataka kuwatoeni katika nchi yenu kwa uchawi wake, sasa mna shauri nini?

قَالُوْۤا اَرْجِهْ وَاَخَاهُ وَابْعَثْ فِی الْمَدَآىِٕنِ حٰشِرِیْنَ ﴿۳۷﴾ۙ

37. Wakasema: Mpe muda yeye na nduguye na uwatume katika miji wakusanyao.

یَاْتُوْكَ بِكُلِّ سَحَّارٍ عَلِیْمٍ ﴿۳۸﴾

38. Watakuletea kila mchawi mkubwa ajuaye.

فَجُمِعَ السَّحَرَةُ لِمِیْقَاتِ یَوْمٍ مَّعْلُوْمٍ ﴿۳۹﴾ۙ

39. Basi walikusanywa wachawi kwa wakati hasa wa siku maalum.

وَّقِیْلَ لِلنَّاسِ هَلْ اَنْتُمْ مُّجْتَمِعُوْنَ ﴿۴۰﴾ۙ

40. Na wakaambiwa watu: Je, nanyi pia mtakusanyika?

لَعَلَّنَا نَتَّبِعُ السَّحَرَةَ اِنْ كَانُوْا هُمُ الْغٰلِبِیْنَ ﴿۴۱﴾

41. Huenda tutawafuata wachawi wakiwa ndio washindao.

فَلَمَّا جَآءَ السَّحَرَةُ قَالُوْا لِفِرْعَوْنَ اَىِٕنَّ لَنَا لَاَجْرًا اِنْ كُنَّا نَحْنُ الْغٰلِبِیْنَ ﴿۴۲﴾

42. Basi walipofika wachawi, wakamwambia Firauni: Je, tutapata ujira tukiwa sisi washindao?

قَالَ نَعَمْ وَاِنَّكُمْ اِذًا لَّمِنَ الْمُقَرَّبِیْنَ ﴿۴۳﴾

43. Akasema: Naam, na kwa yakini kisha mtakuwa miongoni mwa (watu wangu) wa karibu.

قَالَ لَهُمْ مُّوْسٰۤی اَلْقُوْا مَاۤ اَنْتُمْ مُّلْقُوْنَ ﴿۴۴﴾

44. Musa akawaambia tupeni mnavyotaka kuvitupa.

Aya 42. Inaonyesha ya kuwa wachawi wa Firauni walimwuliza: Je, kama tukishinda tutapata ujira? Na walipotupa kamba zao walisema kwa majivuno, *Kwa nguvu za Firauni hakika sisi ndio washindao* (Aya 45). Lakini walipoona mwujiza wa Nabii Musa, mara imani ilipenya

فَاَلْقَوْا حِبَالَهُمْ وَعِصِيَّهُمْ وَقَالُوْا بِعِزَّةِ
فِرْعَوْنَ اِنَّا لَنَحْنُ الْغٰلِبُوْنَ ﴿٤٤﴾

45. Basi wakatupa kamba zao na fimbo zao, na wakasema: Kwa heshima ya Firauni hakika sisi ndio washindao.

فَاَلْقٰى مُوْسٰى عَصَاهُ فَاِذَا هِيَ تَلْقَفُ
مَا يَاْفِكُوْنَ ﴿٤٥﴾

46. Kisha Musa akatupa fimbo yake, nayo mara ikavimeza walivyovizusha.

فَاُلْقِيَ السَّحَرَةُ سٰجِدِيْنَ ﴿٤٦﴾

47. Ndipo wachawi wakainamishwa kusujudu.

قَالُوْٓا اٰمَنَّا بِرَبِّ الْعٰلَمِيْنَ ﴿٤٧﴾

48. Wakasema: Tumemwamini Mola wa walimwengu.

رَبِّ مُوْسٰى وَهٰرُوْنَ ﴿٤٨﴾

49. Mola wa Musa na Harun.

قَالَ اٰمَنْتُمْ لَهٗ قَبْلَ اَنْ اٰذَنَ لَكُمْ ۚ اِنَّهٗ
لَكَبِيْرُكُمُ الَّذِيْ عَلَّمَكُمُ السِّحْرَ ۚ
فَلَسَوْفَ تَعْلَمُوْنَ ۙ لَاُقَطِّعَنَّ اَيْدِيَكُمْ
وَاَرْجُلَكُمْ مِّنْ خِلَافٍ وَّلَاُوصَلِّبَنَّكُمْ
اَجْمَعِيْنَ ﴿٤٩﴾

50. (Firauni) akasema: Je, mmemwamini kabla sijawaruhusuni? Bila shaka yeye ni mkubwa wenu ambaye amewafundisheni uchawi, basi hakika ninyi karibuni mtajua; kwa yakini nitaikata mikono yenu na miguu yenu kwa upande tofauti, na bila shaka nitakufishieni nyote msalabani .

قَالُوْا لَا ضَيْرَ ۚ اِنَّآ اِلٰى رَبِّنَا مُنْقَلِبُوْنَ ﴿٥٠﴾

51. Wakasema: Haidhuru, hakika sisi (sote) ni wenye kurejea kwa Mola wetu.

اِنَّا نَطْمَعُ اَنْ يَّغْفِرَ لَنَا رَبُّنَا خَطٰيٰنَآ اَنْ
كُنَّآ اَوَّلَ الْمُؤْمِنِيْنَ ﴿٥١﴾ ع ٤ ٧

52. Bila shaka sisi tunatumai ya kwamba Mola wetu Atatusamehe makosa yetu, maana sisi tumekuwa wa mwanzo wa waaminio.

FUNGU 4

وَاَوْحَيْنَآ اِلٰى مُوْسٰٓى اَنْ اَسْرِ بِعِبَادِيْٓ
اِنَّكُمْ مُّتَّبَعُوْنَ ﴿٥٢﴾

53. Na Tulimfunulia Musa ya kwamba nenda na watumishi Wangu wakati wa usiku, bila shaka ninyi mtafuatwa.

---

kwa nguvu katika mioyo yao na wakakubali dini ya Nabii Musa. Na Firauni alipokasirika akawakemea kuwa atawakata mikono na miguu, hawakumjali wakamjibu, *Haidhuru*. Hivi ndivyo ilivyo nguvu ya imani, mara ikiingia moyoni inambadilisha mtu kabisa.

Aya 53. *Bila shaka ninyi mtafuatwa*. Maadui wa Nabii Musa walipomfuata alipotoka waliangamia. Namna hii hii maadui wa Mtume *s.a.w.* waliangamizwa walipomfuata Mtume *s.a.w.* Madina.

فَاَرْسَلَ فِرْعَوْنُ فِي الْمَدَآئِنِ حٰشِرِيْنَ ﴿٥٤﴾

54. Basi Firauni akawatuma wakusanyao katika miji:

اِنَّ هٰٓؤُلَآءِ لَشِرْذِمَةٌ قَلِيْلُوْنَ ﴿٥٥﴾

55. Hakika hawa ni kikosi kidogo,

وَاِنَّهُمْ لَنَا لَغَآئِظُوْنَ ﴿٥٦﴾

56. Na bila shaka hao ndio wanaotukasirisha,

وَاِنَّا لَجَمِيْعٌ حٰذِرُوْنَ ﴿٥٧﴾

57. Na hakika sisi sote ni wenye kujihadhari.

فَاَخْرَجْنٰهُمْ مِّنْ جَنّٰتٍ وَّعُيُوْنٍ ﴿٥٨﴾

58. Basi Tukawatoa katika mabustani na chemchem.

وَّكُنُوْزٍ وَّمَقَامٍ كَرِيْمٍ ﴿٥٩﴾

59. Na (katika) mahazina na mahali penye heshima.

كَذٰلِكَ ؕ وَاَوْرَثْنٰهَا بَنِيْٓ اِسْرَآءِيْلَ ﴿٦٠﴾

60. Ndivyo hivyo. Na tukavirithisha kwa wana wa Israeli.

فَاَتْبَعُوْهُمْ مُّشْرِقِيْنَ ﴿٦١﴾

61. Kisha wakawafuata lilipotoka jua.

فَلَمَّا تَرَآءَ الْجَمْعٰنِ قَالَ اَصْحٰبُ مُوْسٰٓى اِنَّا لَمُدْرَكُوْنَ ﴿٦٢﴾

62. Basi yalipoonana majeshi mawili, watu wa Musa wakasema: Hakika tumekamatwa.

قَالَ كَلَّا ۚ اِنَّ مَعِيَ رَبِّيْ سَيَهْدِيْنِ ﴿٦٣﴾

63. (Musa) akasema: La, kwa yakini Mola wanguYu pamoja nami, bila shaka Ataniongoza.

فَاَوْحَيْنَآ اِلٰى مُوْسٰٓى اَنِ اضْرِبْ بِّعَصَاكَ الْبَحْرَ ؕ فَانْفَلَقَ فَكَانَ كُلُّ فِرْقٍ كَالطَّوْدِ الْعَظِيْمِ ﴿٦٤﴾

64. Mara Tulimfunulia Musa: Piga bahari kwa fimbo yako. Basi ikatengana, na kila sehemu ikawa kama mlima mkubwa wa mchanga.

وَاَزْلَفْنَا ثَمَّ الْاٰخَرِيْنَ ﴿٦٥﴾

65. Na Tukawafanya wengine wapakaribie mahali pale.

وَاَنْجَيْنَا مُوْسٰى وَمَنْ مَّعَهٗٓ اَجْمَعِيْنَ ﴿٦٦﴾

66. Na Tukamwokoa Musa na wale waliokuwa pamoja naye wote,

ثُمَّ اَغْرَقْنَا الْاٰخَرِيْنَ ﴿٦٧﴾

67. Kisha Tukawagharikisha wengine.

اِنَّ فِيْ ذٰلِكَ لَاٰيَةً ؕ وَمَا كَانَ اَكْثَرُهُمْ مُّؤْمِنِيْنَ ﴿٦٨﴾

68. Hakika katika hayo imo Ishara, lakini wengi wao si wenye kuamini.

وَاِنَّ رَبَّكَ لَهُوَ الْعَزِيْزُ الرَّحِيْمُ ﴿٦٩﴾ ع ١٧ ٨

69. Na kwa yakini Mola wako ndiye Mwenye ushindi kamili, Mwenye rehema.

FUNGU 5

وَاتْلُ عَلَيْهِمْ نَبَاَ اِبْرٰهِيْمَ ۝٧٠ وقف لازم

70. Na uwasomee habari za Ibrahimu.

اِذْ قَالَ لِاَبِيْهِ وَقَوْمِهٖ مَا تَعْبُدُوْنَ ۝٧١

71. Alipomwambia baba yake na kaumu yake: Mnaabudu nini?

قَالُوْا نَعْبُدُ اَصْنَامًا فَنَظَلُّ لَهَا عٰكِفِيْنَ ۝٧٢

72. Wakasema: Tunaabudu masanamu, nasi tutaendelea kuyafuata.

قَالَ هَلْ يَسْمَعُوْنَكُمْ اِذْ تَدْعُوْنَ ۝٧٣ لا

73. Akasema: Je, yanakusikieni mnapoyaita?

اَوْ يَنْفَعُوْنَكُمْ اَوْ يَضُرُّوْنَ ۝٧٤

74. Au yanawafaeni au yanawadhuruni?

قَالُوْا بَلْ وَجَدْنَآ اٰبَآءَنَا كَذٰلِكَ يَفْعَلُوْنَ ۝٧٥

75. Wakasema: Lakini tumewakuta baba zetu wakifanya vivi hivi.

قَالَ اَفَرَءَيْتُمْ مَّا كُنْتُمْ تَعْبُدُوْنَ ۝٧٦ لا

76. Akasema: Je, mmetafakari juu ya kile mlichokuwa mkikiabudu?

اَنْتُمْ وَاٰبَآؤُكُمُ الْاَقْدَمُوْنَ ۝٧٧ ج

77. Ninyi na baba zenu waliotangulia?

فَاِنَّهُمْ عَدُوٌّ لِّيْٓ اِلَّا رَبَّ الْعٰلَمِيْنَ ۝٧٨ لا

78. Bila shaka hao ni adui zangu ila Mola wa walimwengu,

الَّذِيْ خَلَقَنِيْ فَهُوَ يَهْدِيْنِ ۝٧٩ لا

79. Ambaye ameniumba, naye Ananiongoza,

وَالَّذِيْ هُوَ يُطْعِمُنِيْ وَيَسْقِيْنِ ۝٨٠ لا

80. Naye ndiye Anayenilisha na kuninywesha,

وَاِذَا مَرِضْتُ فَهُوَ يَشْفِيْنِ ۝٨١ ج

81. Na ninapougua basi yeye ananiponya,

وَالَّذِيْ يُمِيْتُنِيْ ثُمَّ يُحْيِيْنِ ۝٨٢ لا

82. Na Ambaye Atanifisha kisha Atanihuisha,

وَالَّذِيْٓ اَطْمَعُ اَنْ يَّغْفِرَ لِيْ خَطِيْٓـَٔتِيْ يَوْمَ الدِّيْنِ ۝٨٣ ط

83. Na ndiye ninayemtumaini kwamba Atanisamehe makosa yangu siku ya Malipo.

رَبِّ هَبْ لِيْ حُكْمًا وَّاَلْحِقْنِيْ بِالصّٰلِحِيْنَ ۝٨٤ لا

84. Mola wangu, Unipe (nguvu ya kutoa) hukumu na Uniunge pamoja na watendao mema.

Aya 75. Siyo jambo la ajabu? Katika mambo ya kidunia watu kila siku wanashika mambo mapya na kuacha ya zamani, lakini katika mambo ya dini wanasema ati wanawafuata baba zao. Je, si hoja ya uwongo hii?

وَاجْعَلْ لِّيْ لِسَانَ صِدْقٍ فِي الْاٰخِرِيْنَ ﴿٨٥﴾

85. Na unijaalie kutajwa kwa wema katika watu wa baadaye.

وَاجْعَلْنِيْ مِنْ وَّرَثَةِ جَنَّةِ النَّعِيْمِ ﴿٨٦﴾

86. Na Unijaalie katika warithi wa Bustani za neema.

وَاغْفِرْ لِاَبِيْٓ اِنَّهٗ كَانَ مِنَ الضَّآلِّيْنَ ﴿٨٧﴾

87. Umsamehe baba yangu, bila shaka yeye yu miongoni mwa waliopotea.

وَلَا تُخْزِنِيْ يَوْمَ يُبْعَثُوْنَ ﴿٨٨﴾

88. Wala usinifedheheshe siku watakayofufuliwa.

يَوْمَ لَا يَنْفَعُ مَالٌ وَّلَا بَنُوْنَ ﴿٨٩﴾

89. Siku ambayo haitafaa mali wala watoto,

اِلَّا مَنْ اَتَى اللّٰهَ بِقَلْبٍ سَلِيْمٍ ﴿٩٠﴾

90. Isipokuwa ajaye kwa Allah na moyo wa utii.

وَاُزْلِفَتِ الْجَنَّةُ لِلْمُتَّقِيْنَ ﴿٩١﴾

91. Na Pepo itasogezwa karibu kwa wacha Mungu.

وَبُرِّزَتِ الْجَحِيْمُ لِلْغٰوِيْنَ ﴿٩٢﴾

92. Na Jahannam itadhihirishwa kwa waasi.

وَقِيْلَ لَهُمْ اَيْنَمَا كُنْتُمْ تَعْبُدُوْنَ ﴿٩٣﴾

93. Na wataambiwa: Wako wapi mliokuwa mkiwaabudu,

مِنْ دُوْنِ اللّٰهِ ۭ هَلْ يَنْصُرُوْنَكُمْ اَوْ يَنْتَصِرُوْنَ ﴿٩٤﴾

94. Badala ya Allah, je, wanaweza kuwasaidieni au kujilipizia kisasi?

فَكُبْكِبُوْا فِيْهَا هُمْ وَالْغَاوٗنَ ﴿٩٥﴾

95. Basi watatupwa humo wao na waasi (wengine).

وَجُنُوْدُ اِبْلِيْسَ اَجْمَعُوْنَ ﴿٩٦﴾

96. Na majeshi ya Ibilisi, wote,

قَالُوْا وَهُمْ فِيْهَا يَخْتَصِمُوْنَ ﴿٩٧﴾

97. Watasema: na hali wakigombana humo:

تَاللّٰهِ اِنْ كُنَّا لَفِيْ ضَلٰلٍ مُّبِيْنٍ ﴿٩٨﴾

98. Wallahi, kwa yakini tulikuwa katika upotevu waziwazi.

اِذْ نُسَوِّيْكُمْ بِرَبِّ الْعٰلَمِيْنَ ﴿٩٩﴾

99. Tulipokuwa tukiwafanyeni sawa na Mwumba wa walimwengu.

وَمَآ اَضَلَّنَآ اِلَّا الْمُجْرِمُوْنَ ﴿١٠٠﴾

100. Na hawakutupoteza ila wakosefu.

فَمَا لَنَا مِنْ شَافِعِيْنَ ﴿١٠١﴾

101. Basi hatuna waombezi.

وَلَا صَدِيْقٍ حَمِيْمٍ ﴿١٠٢﴾

102. Wala rafiki halisi.

فَلَوْ اَنَّ لَنَا كَرَّةً فَنَكُوْنَ مِنَ الْمُؤْمِنِيْنَ ﴿١٠٣﴾

103. Basi kama tungalikuwa na marejeo tungekuwa miongoni mwa waaminio.

اِنَّ فِيْ ذٰلِكَ لَاٰيَةً ؕ وَمَا كَانَ اَكْثَرُهُمْ مُّؤْمِنِيْنَ ﴿١٠٤﴾

104. Bila shaka katika hayo imo Ishara, lakini wengi wao si wenye kuamini.

وَ اِنَّ رَبَّكَ لَهُوَ الْعَزِيْزُ الرَّحِيْمُ ﴿١٠٥﴾ ع ٦

105. Na kwa yakini Mola wako ndiye Mwenye nguvu, Mwenye rehema.

FUNGU 6

كَذَّبَتْ قَوْمُ نُوْحِ ِۨالْمُرْسَلِيْنَ ﴿١٠٦﴾

106. Watu wa Nuhu waliwakadhibisha Mitume.

اِذْ قَالَ لَهُمْ اَخُوْهُمْ نُوْحٌ اَلَا تَتَّقُوْنَ ﴿١٠٧﴾ ج

107. Alipowaambia ndugu yao Nuhu: Je, hamtaogopa?

اِنِّيْ لَكُمْ رَسُوْلٌ اَمِيْنٌ ﴿١٠٨﴾ لا

108. Hakika mimi kwenu ni Mtume mwaminifu.

فَاتَّقُوا اللّٰهَ وَ اَطِيْعُوْنِ ﴿١٠٩﴾ ج

109. Basi Mcheni Allah na mnitii.

وَمَاۤ اَسْـَٔلُكُمْ عَلَيْهِ مِنْ اَجْرٍ ۚ اِنْ اَجْرِيَ اِلَّا عَلٰى رَبِّ الْعٰلَمِيْنَ ﴿١١٠﴾ ج

110. Na siwaombeni juu yake ujira, ujira wangu hauko ila kwa Mola wa walimwengu.

فَاتَّقُوا اللّٰهَ وَ اَطِيْعُوْنِ ﴿١١١﴾ ط

111. Basi Mcheni Allah na nitiini.

قَالُوْۤا اَنُؤْمِنُ لَكَ وَاتَّبَعَكَ الْاَرْذَلُوْنَ ﴿١١٢﴾ ط

112. Wakasema: Je, tukuamini wewe hali wanyonge ndio wanaokufuata?

قَالَ وَمَا عِلْمِيْ بِمَا كَانُوْا يَعْمَلُوْنَ ﴿١١٣﴾ ج

113. Akasema: Siyajui waliyokuwa wakiyatenda.

اِنْ حِسَابُهُمْ اِلَّا عَلٰى رَبِّيْ لَوْ تَشْعُرُوْنَ ﴿١١٤﴾ ج

114. Hesabu yao haiko ila kwa Mola wangu tu, laiti mngetambua.

وَمَاۤ اَنَا بِطَارِدِ الْمُؤْمِنِيْنَ ﴿١١٥﴾ ج

115. Wala mimi sitawafukuza waaminio.

اِنْ اَنَا اِلَّا نَذِيْرٌ مُّبِيْنٌ ﴿١١٦﴾ ط

116. Mimi si ye yote ila ni Mwonyaji dhahiri.

قَالُوْا لَئِنْ لَّمْ تَنْتَهِ يٰنُوْحُ لَتَكُوْنَنَّ مِنَ الْمَرْجُوْمِيْنَ ﴿١١٧﴾ ط

117. Wakasema: Kama hutaacha, ewe Nuhu, bila shaka utakuwa miongoni mwa wanaopigwa mawe.

قَالَ رَبِّ اِنَّ قَوْمِيْ كَذَّبُوْنِ ﴿١١٨﴾ ف

118. Akasema: Mola wangu, bila shaka kaumu yangu wamenikadhibisha.

فَافْتَحْ بَيْنِيْ وَبَيْنَهُمْ فَتْحًا وَّنَجِّنِيْ وَمَنْ مَّعِيَ مِنَ الْمُؤْمِنِيْنَ ﴿١١٩﴾

119. Basi uhukumu baina yangu na baina yao hukumu (nzuri) na Uniokoe mimi na walio pamoja nami walio waaminio.

فَاَنْجَيْنٰهُ وَمَنْ مَّعَهٗ فِي الْفُلْكِ الْمَشْحُوْنِ ﴿١٢٠﴾

120. Kwa hiyo Tukamwokoa yeye na waliokuwa pamoja naye katika merikebu iliyosheheni.

ثُمَّ اَغْرَقْنَا بَعْدُ الْبٰقِيْنَ ﴿١٢١﴾

121. Kisha Tukawagharikisha baadaye waliobaki.

اِنَّ فِيْ ذٰلِكَ لَاٰيَةً ؕ وَمَا كَانَ اَكْثَرُهُمْ مُّؤْمِنِيْنَ ﴿١٢٢﴾

122. Bila shaka katika hayo imo Ishara, lakini wengi wao hawakuwa waaminio.

وَاِنَّ رَبَّكَ لَهُوَ الْعَزِيْزُ الرَّحِيْمُ ﴿١٢٣﴾ ع ١٨ ١٠

123. Na hakika Mola wako ndiye Mwenye ushindi kamili, Mwenye rehema.

FUNGU 7

كَذَّبَتْ عَادُ ِۨالْمُرْسَلِيْنَ ﴿١٢٤﴾

124. Waadi waliwakadhibisha Mitume.

اِذْ قَالَ لَهُمْ اَخُوْهُمْ هُوْدٌ اَلَا تَتَّقُوْنَ ﴿١٢٥﴾

125. Alipowaambia ndugu yao, Hudi: Je, hamtaogopa?

اِنِّيْ لَكُمْ رَسُوْلٌ اَمِيْنٌ ﴿١٢٦﴾

126. Bila shaka mimi kwenu ni Mtume mwaminifu.

فَاتَّقُوا اللّٰهَ وَاَطِيْعُوْنِ ﴿١٢٧﴾

127. Basi Mcheni Allah na nitiini.

وَمَاۤ اَسْـَٔلُكُمْ عَلَيْهِ مِنْ اَجْرٍ ۚ اِنْ اَجْرِيَ اِلَّا عَلٰى رَبِّ الْعٰلَمِيْنَ ﴿١٢٨﴾

128. Wala siwaombeni juu yake ujira, ujira wangu hauko ila kwa Mola wa walimwengu.

اَتَبْنُوْنَ بِكُلِّ رِيْعٍ اٰيَةً تَعْبَثُوْنَ ﴿١٢٩﴾

129. Je, mnajijengea kila palipoinuka alama? Ni bure mnayoyafanya.

وَتَتَّخِذُوْنَ مَصَانِعَ لَعَلَّكُمْ تَخْلُدُوْنَ ﴿١٣٠﴾

130. Na mnajijengea viwanda (vya aina mbali mbali) ili mkae milele.

وَاِذَا بَطَشْتُمْ بَطَشْتُمْ جَبَّارِيْنَ ﴿١٣١﴾

131. Na mnaposhika mnashika kwa jeuri.

فَاتَّقُوا اللّٰهَ وَاَطِيْعُوْنِ ﴿١٣٢﴾

132. Basi Mcheni Allah na nitiini.

وَاتَّقُوا الَّذِيْٓ اَمَدَّكُمْ بِمَا تَعْلَمُوْنَ ﴿١٣٣﴾

133. Na Mcheni Ambaye Amewasaidieni kwa yale mnayoyajua;

اَمَدَّكُمْ بِاَنْعَامٍ وَّبَنِيْنَ ﴿١٣٤﴾

134. Amewasaidieni kwa wanyama na watoto,

وَجَنّٰتٍ وَّعُيُوْنٍ ﴿١٣٥﴾

135. Na Mabustani na chemchem.

اِنِّيْٓ اَخَافُ عَلَيْكُمْ عَذَابَ يَوْمٍ عَظِيْمٍ ﴿١٣٦﴾

136. Hakika ninawahofieni adhabu ya siku kubwa.

قَالُوْا سَوَآءٌ عَلَيْنَآ اَوَعَظْتَ اَمْ لَمْ تَكُنْ مِّنَ الْوٰعِظِيْنَ ﴿١٣٧﴾

137. Wakasema: Ni mamoja kwetu ukitupa mawaidha au kutokuwa miongoni mwa watoao mawaidha.

اِنْ هٰذَآ اِلَّا خُلُقُ الْاَوَّلِيْنَ ﴿١٣٨﴾

138. Haya si cho chote ila ni tabia za watu wa kale.

وَمَا نَحْنُ بِمُعَذَّبِيْنَ ﴿١٣٩﴾

139. Wala sisi hatutaadhibiwa.

فَكَذَّبُوْهُ فَاَهْلَكْنٰهُمْ ؕ اِنَّ فِيْ ذٰلِكَ لَاٰيَةً ؕ وَمَا كَانَ اَكْثَرُهُمْ مُّؤْمِنِيْنَ ﴿١٤٠﴾

140. Basi wakamkadhibisha na Tukawahilikisha; bila shaka katika hayo imo Ishara, lakini wengi wao hawakuwa waaminio.

وَاِنَّ رَبَّكَ لَهُوَ الْعَزِيْزُ الرَّحِيْمُ ﴿١٤١﴾ ع ١١

141. Na kwa yakini Mola wako ndiye Mwenye ushindi kamili, Mwenye rehema.

FUNGU 8

كَذَّبَتْ ثَمُوْدُ الْمُرْسَلِيْنَ ﴿١٤٢﴾

142. Wathamudi waliwakadhibisha Mitume.

اِذْ قَالَ لَهُمْ اَخُوْهُمْ صٰلِحٌ اَلَا تَتَّقُوْنَ ﴿١٤٣﴾

143. Alipowaambia ndugu yao Saleh, Je, hamwogopi?

اِنِّيْ لَكُمْ رَسُوْلٌ اَمِيْنٌ ﴿١٤٤﴾

144. Bila shaka mimi kwenu ni Mtume mwaminifu.

فَاتَّقُوا اللّٰهَ وَاَطِيْعُوْنِ ﴿١٤٥﴾

145. Basi Mcheni Allah na nitiini.

وَمَآ اَسْـَٔلُكُمْ عَلَيْهِ مِنْ اَجْرٍ ۚ اِنْ اَجْرِيَ اِلَّا عَلٰى رَبِّ الْعٰلَمِيْنَ ﴿١٤٦﴾

146. Wala siwaombeni ujira juu yake, ujira wangu hauko ila kwa Mola wa walimwengu.

اَتُتْرَكُوْنَ فِيْ مَا هٰهُنَآ اٰمِنِيْنَ ﴿١٤٧﴾

147. Je, mtaachwa salama katika haya yaliyopo hapa-

فِيْ جَنّٰتٍ وَّعُيُوْنٍ ﴿١٤٨﴾

148. Katika mabustani na chemchem,

وَّزُرُوْعٍ وَّنَخْلٍ طَلْعُهَا هَضِيْمٌ ﴿١٤٩﴾

149. Na mashamba ya nafaka na mitende yenye makole mazito kiasi cha kutaka kudondoka.

وَتَنْحِتُوْنَ مِنَ الْجِبَالِ بُيُوْتًا فٰرِهِيْنَ ﴿١٥٠﴾

150. Na mnachonga milimani majumba kwa ustadi.

فَاتَّقُوا اللّٰهَ وَاَطِيْعُوْنِ ﴿١٥١﴾

151. Basi Mcheni Allah na nitiini.

وَلَا تُطِيْعُوْٓا اَمْرَ الْمُسْرِفِيْنَ ﴿١٥٢﴾

152. Wala msitii amri za wapitao kiasi,

الَّذِيْنَ يُفْسِدُوْنَ فِي الْاَرْضِ وَلَا يُصْلِحُوْنَ ﴿١٥٣﴾

153. Ambao wanafanya uharibifu katika ardhi wala hawasuluhishi.

قَالُوْٓا اِنَّمَآ اَنْتَ مِنَ الْمُسَحَّرِيْنَ ﴿١٥٤﴾

154. Wakasema: Hakika wewe u miongoni mwa waliologwa.

مَآ اَنْتَ اِلَّا بَشَرٌ مِّثْلُنَا ۖ فَاْتِ بِاٰيَةٍ اِنْ كُنْتَ مِنَ الصّٰدِقِيْنَ ﴿١٥٥﴾

155. Wewe si cho chote ila ni mtu kama sisi, basi lete Ishara ikiwa u miongoni mwa wasemao kweli.

قَالَ هٰذِهٖ نَاقَةٌ لَّهَا شِرْبٌ وَّلَكُمْ شِرْبُ يَوْمٍ مَّعْلُوْمٍ ﴿١٥٦﴾

156. Akasema: Huyu ngamia jike awe na zamu yake ya kunywa, na ninyi muwe na zamu yenu ya kunywa katika siku maalumu.

وَلَا تَمَسُّوْهَا بِسُوْٓءٍ فَيَاْخُذَكُمْ عَذَابُ يَوْمٍ عَظِيْمٍ ﴿١٥٧﴾

157. Wala msimguse kwa ubaya isije ikawashikeni adhabu ya siku kubwa.

فَعَقَرُوْهَا فَاَصْبَحُوْا نٰدِمِيْنَ ﴿١٥٨﴾

158. Lakini wao walimkata miguu na wakawa wenye kujuta.

فَاَخَذَهُمُ الْعَذَابُ ۗ اِنَّ فِيْ ذٰلِكَ لَاٰيَةً ۗ وَمَا كَانَ اَكْثَرُهُمْ مُّؤْمِنِيْنَ ﴿١٥٩﴾

159. Basi adhabu ikawashika. Bila shaka katika hayo imo Ishara, lakini wengi wao hawakuwa waaminio.

وَاِنَّ رَبَّكَ لَهُوَ الْعَزِيْزُ الرَّحِيْمُ ﴿١٦٠﴾ ع ١٣

160. Na hakika Mola wako ndiye Mshindi kamili, Mwenye rehema.

FUNGU 9

كَذَّبَتْ قَوْمُ لُوْطِ ِۨالْمُرْسَلِيْنَ ﴿١٦١﴾

161. Watu wa Luti waliwakadhibisha Mitume.

اِذْ قَالَ لَهُمْ اَخُوْهُمْ لُوْطٌ اَلَا تَتَّقُوْنَ ﴿١٦٢﴾

162. Alipowaambia ndugu yao Luti: Je, hamwogopi?

اِنِّيْ لَكُمْ رَسُوْلٌ اَمِيْنٌ ﴿١٦٣﴾

163. Hakika mimi kwenu ni Mtume mwaminifu.

فَاتَّقُوا اللّٰهَ وَاَطِيْعُوْنِ ﴿١٦٤﴾

164. Basi mcheni Allah na nitiini.

وَمَآ اَسْـَٔلُكُمْ عَلَيْهِ مِنْ اَجْرٍ ۚ اِنْ اَجْرِيَ اِلَّا عَلٰى رَبِّ الْعٰلَمِيْنَ ﴿١٦٥﴾

165. Wala siwaombeni ujira juu yake; si ujira wangu ila kwa Mola wa walimwengu.

اَتَاْتُوْنَ الذُّكْرَانَ مِنَ الْعٰلَمِيْنَ ﴿١٦٦﴾

166. Je, mnawaingilia wanaume katika viumbe,

وَتَذَرُوْنَ مَا خَلَقَ لَكُمْ رَبُّكُمْ مِّنْ اَزْوَاجِكُمْ ۭ بَلْ اَنْتُمْ قَوْمٌ عٰدُوْنَ ﴿١٦٧﴾

167. Na mnawaacha Aliowaumbieni Mola wenu katika wake zenu? Kweli ninyi ni watu warukao mipaka.

قَالُوْا لَىِٕنْ لَّمْ تَنْتَهِ يٰلُوْطُ لَتَكُوْنَنَّ مِنَ الْمُخْرَجِيْنَ ﴿١٦٨﴾

168. Wakasema: kama usipoacha, ee Luti, bila shaka utakuwa miongoni mwa wanaofukuzwa.

قَالَ اِنِّىْ لِعَمَلِكُمْ مِّنَ الْقَالِيْنَ ﴿١٦٩﴾

169. Akasema: Kwa yakini mimi ni katika wale wachukiao sana matendo yenu.

رَبِّ نَجِّنِيْ وَاَهْلِيْ مِمَّا يَعْمَلُوْنَ ﴿١٧٠﴾

170. Mola wangu, Uniokoe mimi na ahali zangu katika yale wanayoyafanya.

فَنَجَّيْنٰهُ وَاَهْلَهٗٓ اَجْمَعِيْنَ ﴿١٧١﴾

171. Basi Tukamwokoa yeye na watu wake wote.

اِلَّا عَجُوْزًا فِي الْغٰبِرِيْنَ ﴿١٧٢﴾

172. Isipokuwa kikongwe katika wakaao nyuma.

ثُمَّ دَمَّرْنَا الْاٰخَرِيْنَ ﴿١٧٣﴾

173. Kisha Tukawaangamiza wengine.

وَاَمْطَرْنَا عَلَيْهِمْ مَّطَرًا ۚ فَسَاۗءَ مَطَرُ الْمُنْذَرِيْنَ ﴿١٧٤﴾

174. Na Tukawanyeshelezea mvua; basi ni mbaya iliyoje mvua inayowashukia wale walioonywa.

اِنَّ فِيْ ذٰلِكَ لَاٰيَةً ۭ وَمَا كَانَ اَكْثَرُهُمْ مُّؤْمِنِيْنَ ﴿١٧٥﴾

175. Bila shaka katika hayo imo Ishara, lakini wengi wao hawakuwa waaminio.

وَاِنَّ رَبَّكَ لَهُوَ الْعَزِيْزُ الرَّحِيْمُ ﴿١٧٦﴾ ع ١٦ ١٣

176. Na hakika Mola wako ndiye Mshindi kamili, Mwenye rehema.

Aya 172. *Kikongwe* anayetajwa hapa alikuwa mke wa Nabii Luti.

FUNGU 10

كَذَّبَ اَصۡحٰبُ لۡـَٔيۡكَةِ الۡمُرۡسَلِيۡنَ ۚ﴿۱۷۷﴾

177. Watu wa mwituni waliwakadhibisha Mitume.

اِذۡ قَالَ لَهُمۡ شُعَيۡبٌ اَلَا تَتَّقُوۡنَ ۚ﴿۱۷۸﴾

178. Alipowaambia Shuaibu: Je, hamwogopi?

اِنِّىۡ لَـكُمۡ رَسُوۡلٌ اَمِيۡنٌ ۙ﴿۱۷۹﴾

179. Hakika mimi kwenu ni Mtume mwaminifu.

فَاتَّقُوا اللّٰهَ وَاَطِيۡعُوۡنِ ۚ﴿۱۸۰﴾

180. Basi mcheni Allah na nitiini.

وَمَاۤ اَسۡـَٔـلُكُمۡ عَلَيۡهِ مِنۡ اَجۡرٍ ۚ اِنۡ اَجۡرِىَ اِلَّا عَلٰى رَبِّ الۡعٰلَمِيۡنَ ۖ﴿۱۸۱﴾

181. Wala siwaombeni ujira juu yake, ujira wangu ni kwa Mola wa walimwengu tu.

اَوۡفُوا الۡكَيۡلَ وَلَا تَكُوۡنُوۡا مِنَ الۡمُخۡسِرِيۡنَ ۚ﴿۱۸۲﴾

182. Kijazeni kipimo sawasawa wala msiwe miongoni mwa wapunjao.

وَزِنُوۡا بِالۡقِسۡطَاسِ الۡمُسۡتَقِيۡمِ ۚ﴿۱۸۳﴾

183. Na pimeni kwa mizani iliyo sawa.

وَلَا تَبۡخَسُوا النَّاسَ اَشۡيَآءَهُمۡ وَلَا تَعۡثَوۡا فِى الۡاَرۡضِ مُفۡسِدِيۡنَ ۚ﴿۱۸۴﴾

184. Wala msiwapunguzie watu vitu vyao, wala msitembee katika ardhi mkifanya ufisadi.

وَاتَّقُوا الَّذِىۡ خَلَقَكُمۡ وَالۡجِبِلَّةَ الۡاَوَّلِيۡنَ ۖ﴿۱۸۵﴾

185. Na Mcheni Aliyewaumbeni ninyi na viumbe vilivyoumbwa kwanza.

قَالُوۡۤا اِنَّمَاۤ اَنۡتَ مِنَ الۡمُسَحَّرِيۡنَ ۙ﴿۱۸۶﴾

186. Wakasema: Hakika wewe u miongoni mwa waliologwa.

وَمَاۤ اَنۡتَ اِلَّا بَشَرٌ مِّثۡلُنَا وَاِنۡ نَّظُنُّكَ لَمِنَ الۡكٰذِبِيۡنَ ۚ﴿۱۸۷﴾

187. Nawe siwe ila ni mtu kama sisi; na kwa yakini tunakufahamu u miongoni mwa waongo.

فَاَسۡقِطۡ عَلَيۡنَا كِسَفًا مِّنَ السَّمَآءِ اِنۡ كُنۡتَ مِنَ الصّٰدِقِيۡنَ ۖ﴿۱۸۸﴾

188. Basi tuangushie kipande cha mbingu ikiwa u miongoni mwa wasemao kweli.

قَالَ رَبِّىۡۤ اَعۡلَمُ بِمَا تَعۡمَلُوۡنَ ﴿۱۸۹﴾

189. Akasema: Mola wangu Anajua sana mnayoyatenda.

فَكَذَّبُوۡهُ فَاَخَذَهُمۡ عَذَابُ يَوۡمِ الظُّلَّةِ ؕ اِنَّهٗ كَانَ عَذَابَ يَوۡمٍ عَظِيۡمٍ ﴿۱۹۰﴾

190. Lakini wakamkadhibisha, basi ikawashika adhabu ya siku ya kivuli.

Aya 188. *Kipande cha mbingu* muradi wake ni adhabu.

Aya 190. *Siku ya kivuli,* yaani adhabu iliwafunika kama vile kivuli kinavyofunikiza.

Bila shaka hiyo ilikuwa adhabu ya siku kubwa.

191. Hakika katika hayo imo Ishara, na wengi wao hawakuwa waaminio.

اِنَّ فِیْ ذٰلِكَ لَاٰیَةً ؕ وَمَا كَانَ اَكْثَرُهُمْ مُّؤْمِنِیْنَ ﴿۱۹۱﴾

192. Na kwa yakini Mola wako ndiye Mwenye nguvu, Mwenye rehema.

وَاِنَّ رَبَّكَ لَهُوَ الْعَزِیْزُ الرَّحِیْمُ ﴿۱۹۲﴾ ع

FUNGU 11

193. Na bila shaka hii (Qur'an) ni uteremsho wa Mola wa walimwengu.

وَاِنَّهٗ لَتَنْزِیْلُ رَبِّ الْعٰلَمِیْنَ ﴿۱۹۳﴾

194. Ameteremka nayo roho mwaminifu,

نَزَلَ بِهِ الرُّوْحُ الْاَمِیْنُ ﴿۱۹۴﴾ۙ

195. Juu ya moyo wako ili uwe miongoni mwa Waonyaji,

عَلٰی قَلْبِكَ لِتَكُوْنَ مِنَ الْمُنْذِرِیْنَ ﴿۱۹۵﴾ۙ

196. Kwa lugha ya Kiarabu bayana.

بِلِسَانٍ عَرَبِیٍّ مُّبِیْنٍ ﴿۱۹۶﴾ؕ

197. Na kwa yakini hayo yamo katika Vitabu vya kale.

وَاِنَّهٗ لَفِیْ زُبُرِ الْاَوَّلِیْنَ ﴿۱۹۷﴾

198. Je, haikuwa ishara kubwa kwao kwamba wanaijua (hii Kurani) wanachuoni wa wana wa Israeli?

اَوَلَمْ یَكُنْ لَّهُمْ اٰیَةً اَنْ یَّعْلَمَهٗ عُلَمٰٓؤُا بَنِیْۤ اِسْرَآءِیْلَ ﴿۱۹۸﴾ؕ

199. Na lau tungaliiteremsha kwa asiyekuwa Mwarabu,

وَلَوْ نَزَّلْنٰهُ عَلٰی بَعْضِ الْاَعْجَمِیْنَ ﴿۱۹۹﴾ۙ

200. Na akawasomea, wasingalikuwa wenye kuiamini.

فَقَرَاَهٗ عَلَیْهِمْ مَّا كَانُوْا بِهٖ مُؤْمِنِیْنَ ﴿۲۰۰﴾ؕ

201. Hivyo ndivyo Tulivyoiingiza (kufuru) katika mioyo ya wakosefu.

كَذٰلِكَ سَلَكْنٰهُ فِیْ قُلُوْبِ الْمُجْرِمِیْنَ ﴿۲۰۱﴾ؕ

202. Hawataiamini mpaka waone adhabu iumizayo.

لَا یُؤْمِنُوْنَ بِهٖ حَتّٰی یَرَوُا الْعَذَابَ الْاَلِیْمَ ﴿۲۰۲﴾ۙ

203. Basi itawafikia kwa ghafla hali hawatambui.

فَیَاْتِیَهُمْ بَغْتَةً وَّهُمْ لَا یَشْعُرُوْنَ ﴿۲۰۳﴾ۙ

Aya 194. *Roho mwaminifu* ni Malaika Jibrili.

Aya 197. Muradi ni kwamba bishara za kufika Mtume *s.a.w.* zimo katika vitabu vya zamani kama Taurati (Kumbukumbu 18:18; Isaya 21:18; Zaburi 118:22 n.k.w).

Aya 201. Yaani uzuri wa mafundisho ya Kiislamu uliingia katika mioyo ya wasioamini, lakini kwa sababu za dunia yao hawakutaka kuikubali.

فَيَقُوْلُوْا هَلْ نَحْنُ مُنْظَرُوْنَ ﴿٢٠٤﴾

204. Na watasema: Je, sisi tutapewa muda?

اَفَبِعَذَابِنَا يَسْتَعْجِلُوْنَ ﴿٢٠٥﴾

205. Basi je, wanaihimiza adhabu Yetu?

اَفَرَءَيْتَ اِنْ مَّتَّعْنٰهُمْ سِنِيْنَ ﴿٢٠٦﴾

206. Unaonaje kama Tukiwafaidisha kwa miaka,

ثُمَّ جَآءَهُمْ مَّا كَانُوْا يُوْعَدُوْنَ ﴿٢٠٧﴾

207. Kisha iwafikie (adhabu) waliyokuwa wakiahidiwa?

مَآ اَغْنٰى عَنْهُمْ مَّا كَانُوْا يُمَتَّعُوْنَ ﴿٢٠٨﴾

208. Hayatawafaa yale waliyofaidishwa.

وَمَآ اَهْلَكْنَا مِنْ قَرْيَةٍ اِلَّا لَهَا مُنْذِرُوْنَ ﴿٢٠٩﴾

معانقة عبد المجيد مدني

209. Wala Hatukuuangamiza mji wo wote ila ulikuwa na Waonyaji.

ذِكْرٰى ۛ وَمَا كُنَّا ظٰلِمِيْنَ ﴿٢١٠﴾

210. (Huu ni) ukumbusho mkubwa uonyao; wala Hatukuwa wadhalimu.

وَمَا تَنَزَّلَتْ بِهِ الشَّيٰطِيْنُ ﴿٢١١﴾

211. Wala mashetani hawakuteremka nayo,

وَمَا يَنْۢبَغِيْ لَهُمْ وَمَا يَسْتَطِيْعُوْنَ ﴿٢١٢﴾

212. Wala haiwapasi, na tena hawawezi.

اِنَّهُمْ عَنِ السَّمْعِ لَمَعْزُوْلُوْنَ ﴿٢١٣﴾

213. Bila shaka wao wamezuiliwa kusikia.

فَلَا تَدْعُ مَعَ اللّٰهِ اِلٰهًا اٰخَرَ فَتَكُوْنَ مِنَ الْمُعَذَّبِيْنَ ﴿٢١٤﴾

214. Basi usimwombe mungu mwingine pamoja naAllah waila utakuwa miongoni mwa wanaoadhibiwa.

وَاَنْذِرْ عَشِيْرَتَكَ الْاَقْرَبِيْنَ ﴿٢١٥﴾

215. Na uwaonye jamaa zako wa karibu.

وَاخْفِضْ جَنَاحَكَ لِمَنِ اتَّبَعَكَ مِنَ الْمُؤْمِنِيْنَ ﴿٢١٦﴾

216. Na uinamishe bawa lako kwa yule anayekufuata miongoni mwa waaminio.

فَاِنْ عَصَوْكَ فَقُلْ اِنِّيْ بَرِيْٓءٌ مِّمَّا تَعْمَلُوْنَ ﴿٢١٧﴾

217. Na kama wakikuasi, basi sema: Mimi ni mbali na hayo mnayoyafanya.

Aya 215. Kwa kufuata amri ya Allah iliyomo katika Aya hii, Mtume *s.a.w.* alipanda juu ya kilima Safa na akayaita makabila yote ya Makka kila moja kwa jina lake. Wote walipokusanyika akawauliza, Mwaonaje kama niwaambieni kuwa nyuma ya kilima hiki kuna jeshi kubwa sana la askari linalokuja wapigeni, mtakubali? Wote kwa sauti moja wakajibu, Naam, maana hatujasikia umetamka uwongo. Hapo akawaambia, basi mimi nimetumwa na Allah kuwaonyeni juu ma matokeo mabaya ya matendo yenu. Hapo hapo Abu Lahab, baba yake mdogo, akamwambia, Uangamie, je, kwa mambo haya ndiyo umetuita hapa? (Bukhari).

وَتَوَكَّلْ عَلَى الْعَزِيْزِ الرَّحِيْمِ ﴿٢١٨﴾

218. Na umtegemee Mwenye nguvu, Mwenye rehema.

الَّذِىْ يَرٰىكَ حِيْنَ تَقُوْمُ ﴿٢١٩﴾

219. Ambaye Anakuona unaposimama.

وَتَقَلُّبَكَ فِى السّٰجِدِيْنَ ﴿٢٢٠﴾

220. Na kuwahangaikia kwako wale wanaosujudu.

اِنَّهٗ هُوَ السَّمِيْعُ الْعَلِيْمُ ﴿٢٢١﴾

221. Hakika Yeye ndiye Asikiaye, Ajuaye.

هَلْ اُنَبِّئُكُمْ عَلٰى مَنْ تَنَزَّلُ الشَّيٰطِيْنُ ﴿٢٢٢﴾

222. Je, Niwaambieni ambao mashetani wanawateremkia?

تَنَزَّلُ عَلٰى كُلِّ اَفَّاكٍ اَثِيْمٍ ﴿٢٢٣﴾

223. Wanateremka juu ya kila mzushi mkubwa, mwenye dhambi.

يُّلْقُوْنَ السَّمْعَ وَاَكْثَرُهُمْ كٰذِبُوْنَ ﴿٢٢٤﴾

224. Hutega masikio na wengi wao ni waongo.

وَالشُّعَرَآءُ يَتَّبِعُهُمُ الْغَاوٗنَ ﴿٢٢٥﴾

225. Na watungaji mashairi, waliopotea ndio wanaowafuata.

اَلَمْ تَرَ اَنَّهُمْ فِىْ كُلِّ وَادٍ يَّهِيْمُوْنَ ﴿٢٢٦﴾

226. Je, huoni kwamba wao wanahangaika katika kila bonde,

وَاَنَّهُمْ يَقُوْلُوْنَ مَا لَا يَفْعَلُوْنَ ﴿٢٢٧﴾

227. Na ya kwamba wao wanasema wasiyoyatenda?

اِلَّا الَّذِيْنَ اٰمَنُوْا وَعَمِلُوا الصّٰلِحٰتِ وَذَكَرُوا اللّٰهَ كَثِيْرًا وَّانْتَصَرُوْا مِنْۢ بَعْدِ مَا ظُلِمُوْا ؕ وَسَيَعْلَمُ الَّذِيْنَ ظَلَمُوْٓا اَىَّ مُنْقَلَبٍ يَّنْقَلِبُوْنَ ﴿٢٢٨﴾ ع ١٥

228. Ila wale walioamini, na kufanya vitendo vizuri, na kumkumbuka Allah kwa wingi, na wakalipiza kisasi baada ya kudhulumiwa. Na karibuni wafanyao dhuluma watajua ni mgeuko wa namna gani watakaogeuka.

Aya 224. Kama mafundisho ya Qur'an yametoka kwa Shetani yasingeagiza mambo mazuri-mazuri namna hii, na isitoshe watu wabaya na mashetani wangekuwa tayari kuyafuata na wasingeyafanyia uadui. Kama Nabii s.a.w. angekuwa mwongo, basi mashetani wangefika kwake na wangeleta mambo ya upuuzi, lakini mambo yenye busara na hekima kama yaliyomo katika Qur'an yasingeweza kamwe kutokea kwa Shetani.

Aya 228. Aya hii inaonyesha ya kuwa kuna watunga mashairi ambao husema wanayoyatenda na yaliyo haki. Hao ni waaminio. Wao wamekuwa mbali na wale watunga mashairi wengine waliotajwa katika Aya 225, 226 na 227.

سُوْرَةُ النَّمْلِ مَكِّيَّةٌ وَّ هِيَ مَعَ الْبَسْمَلَةِ اَرْبَعٌ وَّ تِسْعُوْنَ اٰيَةً وَّ سَبْعَةُ رُكُوْعَاتٍ

27. SURA AN-NAML

Imeteremshwa Makka

Ina mafungu 7 na Aya 94 pamona na Bismillahi

بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ ①

1. Kwa jina la Allah, Mwingi wa rehema, Mwingi wa ukarimu.

طٰسٓ ۚ تِلْكَ اٰيٰتُ الْقُرْاٰنِ وَكِتَابٍ مُّبِيْنٍ ۙ②

2. (Allah) Atakasaye, Asikiaye! Hizi ni Aya za Qur'an na za Kitabu kielezacho.

هُدًى وَّ بُشْرٰى لِلْمُؤْمِنِيْنَ ۙ③

3. Mwongozo na habari njema kwa waaminio,

الَّذِيْنَ يُقِيْمُوْنَ الصَّلٰوةَ وَ يُؤْتُوْنَ الزَّكٰوةَ وَهُمْ بِالْاٰخِرَةِ هُمْ يُوْقِنُوْنَ ④

4. Ambao wanasimamisha Sala na kutoa Zaka, nao wana yakini na Akhera.

اِنَّ الَّذِيْنَ لَا يُؤْمِنُوْنَ بِالْاٰخِرَةِ زَيَّنَّا لَهُمْ اَعْمَالَهُمْ فَهُمْ يَعْمَهُوْنَ ؕ⑤

5. Kwa hakika wale wasioiamini Akhera Tumewapambia vitendo vyao, nao wanahangaika ovyo.

اُولٰٓئِكَ الَّذِيْنَ لَهُمْ سُوْٓءُ الْعَذَابِ وَ هُمْ فِي الْاٰخِرَةِ هُمُ الْاَخْسَرُوْنَ ⑥

6. Hao ndio watakaopata adhabu mbaya na hao katika Akhera ndio wapatao hasara zaidi.

وَ اِنَّكَ لَتُلَقَّى الْقُرْاٰنَ مِنْ لَّدُنْ حَكِيْمٍ عَلِيْمٍ ⑦

7. Na hakika wewe unafundishwa Qur'an na Yule Aliye Mwenye hekima, Mjuzi.

اِذْ قَالَ مُوْسٰى لِاَهْلِهٖٓ اِنِّيْٓ اٰنَسْتُ نَارًا ؕ سَاٰتِيْكُمْ مِّنْهَا بِخَبَرٍ اَوْ اٰتِيْكُمْ بِشِهَابٍ قَبَسٍ لَّعَلَّكُمْ تَصْطَلُوْنَ ⑧

8. (Kumbuka) Musa alipowaambia ahali zake: Hakika nimeona moto, sasa hivi nitawaleteeni habari au nitawaleteeni kijinga kiwakacho ili mpate kuota.

Sura hii imepewa jina la kabila la Naml lililotajwa katika Aya 19 kwa kuhusiana na safari ya majeshi ya Nabii Suleimani alipomwendea Malkia wa Sheba. Sura hii pia ilishuka Makka.

Aya 2. *Taa siin.* Haya ni maneno ya mkato kwa ajili ya sifa za Allah. Taa ni Taahir (Atakasaye), Siin ni Samii' (Asikiaye).

Aya 5. *Vitendo vyao* ni vile walivyotakiwa kuvitenda, sivyo vile viovu ambavyo walikuwa wakivitenda.

فَلَمَّا جَآءَهَا نُوْدِیَ اَنْۢ بُوْرِكَ مَنْ
فِی النَّارِ وَمَنْ حَوْلَهَا ؕ وَ سُبْحٰنَ اللّٰهِ
رَبِّ الْعٰلَمِیْنَ ۝٩

9. Basi alipoufikia, ikanadiwa ya kwamba amebarikiwa aliyomo katika moto na aliyoko pembeni mwake; na Ametukuka Allah, Mola wa walimwengu.

یٰمُوْسٰۤی اِنَّهٗۤ اَنَا اللّٰهُ الْعَزِیْزُ الْحَكِیْمُ ۙ ۝١٠

10. Ee Musa, hakika Mimi ndiye Allah, Mwenye nguvu, Mwenye hekima.

وَ اَلْقِ عَصَاكَ ؕ فَلَمَّا رَاٰهَا تَهْتَزُّ
كَاَنَّهَا جَآنٌّ وَّلّٰی مُدْبِرًا وَّ لَمْ یُعَقِّبْ ؕ
یٰمُوْسٰی لَا تَخَفْ ۫ اِنِّیْ لَا یَخَافُ
لَدَیَّ الْمُرْسَلُوْنَ ۝١١

11. Na itupe fimbo yako, lakini alipoiona ikiyumbayumba kama nyoka akageuka kurudi nyuma wala hakungoja: Ee Musa usiogope; bila shaka Mimi Ndiye Yule ambaye hawaogopi mbele yangu Mitume.

اِلَّا مَنْ ظَلَمَ ثُمَّ بَدَّلَ حُسْنًۢا بَعْدَ سُوْٓءٍ
فَاِنِّیْ غَفُوْرٌ رَّحِیْمٌ ۝١٢

12. Ila aliyedhulumu kisha akabadilisha wema baada ya ubaya, basi kwa hakika mimi ni Msamehevu, Mrehemevu.

وَ اَدْخِلْ یَدَكَ فِیْ جَیْبِكَ تَخْرُجْ
بَیْضَآءَ مِنْ غَیْرِ سُوْٓءٍ ؕ فِیْ تِسْعِ اٰیٰتٍ
اِلٰی فِرْعَوْنَ وَ قَوْمِهٖ ؕ اِنَّهُمْ كَانُوْا
قَوْمًا فٰسِقِیْنَ ۝١٣

13. Na ingiza mkono wako kifuani pako ndani ya vazi lako, utatoka mweupe pasipo maradhi. Ni katika Ishara tisa kwa Firauni na watu wake, hakika hao ni watu wenye kuvunja amri.

فَلَمَّا جَآءَتْهُمْ اٰیٰتُنَا مُبْصِرَةً قَالُوْا
هٰذَا سِحْرٌ مُّبِیْنٌ ۝١٤

14. Basi zilipowafikia Ishara Zetu zionyeshazo, wakasema: Huu ni uchawi dhahiri.

وَجَحَدُوْا بِهَا وَ اسْتَیْقَنَتْهَاۤ اَنْفُسُهُمْ
ظُلْمًا وَّ عُلُوًّا ؕ فَانْظُرْ كَیْفَ كَانَ
عَاقِبَةُ الْمُفْسِدِیْنَ ۝١٥

15. Na wakazikataa hali nafsi zao zina yakini nazo, kwa dhuluma na kujivuna. Basi angalia ulikuwaje mwisho wa wafanyao ufisadi!

Aya 9. *Aliyomo katika moto* ni maneno ambayo yanaweza kuwa na makusudio namna mbili: (1)Nabii Musa na *aliyoko pembeni mwake* ni ahali zake. (2) *Aliyomo katika moto* pia muradi wake ni *anayetafuta moto* (Taj-ut-Tafaasiir). Ikumbukwe ya kuwa moto ule haukuwa Mungu.

Aya 13. *Ishara tisa* ni hizi: (1) Fimbo, (2) Mkono mweupe, (3) Tufani, (4) Kufa kwa watoto waliozaliwa kwanza, (5) Nzige, (6) Chawa, (7) vyura, (8) Damu na (9) Njaa (Sura A'raf).

FUNGU 2

16. Na bila shaka Tuliwapa Daudi na Suleimani elimu, na wakasema: Sifa zote njema ni za Allah, Aliyetufadhili kuliko wengi katika watumishi Wake waaminio.

وَ لَقَدْ اٰتَيْنَا دَاوٗدَ وَ سُلَيْمٰنَ عِلْمًا ۚ وَقَالَا الْحَمْدُ لِلّٰهِ الَّذِيْ فَضَّلَنَا عَلٰى كَثِيْرٍ مِّنْ عِبَادِهِ الْمُؤْمِنِيْنَ ﴿١٦﴾

17. Na Suleimani alimrithi Daudi na akasema: Enyi watu! Tumefundishwa usemi wa ndege na tumepewa kila kitu; hakika hii ndiyo fadhili dhahiri.

وَوَرِثَ سُلَيْمٰنُ دَاوٗدَ وَقَالَ يٰۤاَيُّهَا النَّاسُ عُلِّمْنَا مَنْطِقَ الطَّيْرِ وَاُوْتِيْنَا مِنْ كُلِّ شَيْءٍ ؕ اِنَّ هٰذَا لَهُوَ الْفَضْلُ الْمُبِيْنُ ﴿١٧﴾

18. Na alikusanyiwa Suleimani majeshi yake katika majini na watu na ndege, nayo yakawekwa makundi-makundi.

وَحُشِرَ لِسُلَيْمٰنَ جُنُوْدُهٗ مِنَ الْجِنِّ وَالْاِنْسِ وَالطَّيْرِ فَهُمْ يُوْزَعُوْنَ ﴿١٨﴾

19. Hata walipofika katika bonde la Naml akasema mwanamke mmoja Mnamli, "Enyi Wanamli ingieni majumbani mwenu asiwapondeni Suleimani na majeshi yake hali hawatambui.

حَتّٰۤى اِذَاۤ اَتَوْا عَلٰى وَادِ النَّمْلِ ۙ قَالَتْ نَمْلَةٌ يّٰۤاَيُّهَا النَّمْلُ ادْخُلُوْا مَسٰكِنَكُمْ ۚ لَا يَحْطِمَنَّكُمْ سُلَيْمٰنُ وَجُنُوْدُهٗ ۙ وَهُمْ لَا يَشْعُرُوْنَ ﴿١٩﴾

20. Basi akatabasamu akicheka kutokana na kauli yake hii, na akasema: Ee Mola wangu, Unipe nguvu niishukuru neema Yako Uliyonineemesha mimi na wazazi wangu, na nipate kufanya vitendo vizuri vikupendezavyo, na Uniingize kwa rehema Zako katika watumishi Wako wema.

فَتَبَسَّمَ ضَاحِكًا مِّنْ قَوْلِهَا وَقَالَ رَبِّ اَوْزِعْنِيْۤ اَنْ اَشْكُرَ نِعْمَتَكَ الَّتِيْۤ اَنْعَمْتَ عَلَيَّ وَعَلٰى وَالِدَيَّ وَاَنْ اَعْمَلَ صَالِحًا تَرْضٰىهُ وَ اَدْخِلْنِيْ بِرَحْمَتِكَ فِيْ عِبَادِكَ الصّٰلِحِيْنَ ﴿٢٠﴾

21. Na akawakagua ndege na akasema: Nimekuwaje simwoni Hudhud, au amekuwa miongoni mwa wasiokuwapo?

وَتَفَقَّدَ الطَّيْرَ فَقَالَ مَا لِيَ لَاۤ اَرَى الْهُدْهُدَ ۖ اَمْ كَانَ مِنَ الْغَآئِبِيْنَ ﴿٢١﴾

Aya 17. Nabii Dawud alikuwa na watoto 19, lakini aliyerithi elimu yake ni Nabii Suleimani.

Aya 19. *Naml* ni bonde lililoko baina ya Jibrin na Askalan (Tabari).

لَاُعَذِّبَنَّهٗ عَذَابًا شَدِيْدًا اَوْ لَاَاْذْبَحَنَّهٗٓ اَوْ لَيَاْتِيَنِّيْ بِسُلْطٰنٍ مُّبِيْنٍ ﴿٢١﴾

22. Nitamwadhibu adhabu kali au nitamchinja, isipokuwa tu kama aniletee dalili iliyo wazi ya kujitetea.

فَمَكَثَ غَيْرَ بَعِيْدٍ فَقَالَ اَحَطْتُّ بِمَا لَمْ تُحِطْ بِهٖ وَجِئْتُكَ مِنْ سَبَاٍ بِنَبَاٍ يَّقِيْنٍ ﴿٢٢﴾

23. Basi hakungojea sana mara (Hud hud) akasema: Nimeligundua usiloligundua, na nimekuletea kutoka Saba habari zenye yakini.

اِنِّيْ وَجَدْتُّ امْرَاَةً تَمْلِكُهُمْ وَاُوْتِيَتْ مِنْ كُلِّ شَيْءٍ وَّلَهَا عَرْشٌ عَظِيْمٌ ﴿٢٣﴾

24. Hakika nimemkuta mwanamke anayewatawala, naye amepewa sehemu katika kila kitu na anayo enzi kubwa.

وَجَدْتُّهَا وَقَوْمَهَا يَسْجُدُوْنَ لِلشَّمْسِ مِنْ دُوْنِ اللّٰهِ وَزَيَّنَ لَهُمُ الشَّيْطٰنُ اَعْمَالَهُمْ فَصَدَّهُمْ عَنِ السَّبِيْلِ فَهُمْ لَا يَهْتَدُوْنَ ﴿٢٤﴾ۙ

25. Nimemkuta yeye na watu wake wakilisujudia jua badala ya Allah, na Shetani amewapambia vitendo vyao na akawazuilia njia, kwa hiyo hawakuongoka.

اَلَّا يَسْجُدُوْا لِلّٰهِ الَّذِيْ يُخْرِجُ الْخَبْءَ فِي السَّمٰوٰتِ وَالْاَرْضِ وَيَعْلَمُ مَا تُخْفُوْنَ وَمَا تُعْلِنُوْنَ ﴿٢٥﴾

26. Mbona hawamsujudii Allah Ambaye Huyatoa yaliyofichikana katika mbingu na ardhi na Huyajua mnayoyaficha na mnayoyadhihirisha.

اَللّٰهُ لَآ اِلٰهَ اِلَّا هُوَ رَبُّ الْعَرْشِ الْعَظِيْمِ ﴿٢٦﴾ ع

27. Allah, hapana aabudiwaye ila Yeye, Mola wa Enzi kubwa.

قَالَ سَنَنْظُرُ اَصَدَقْتَ اَمْ كُنْتَ مِنَ الْكٰذِبِيْنَ ﴿٢٧﴾

28. Akasema (Suleimani): Tutatazama kama umesema kweli au u miongoni mwa waongo.

اِذْهَبْ بِّكِتٰبِيْ هٰذَا فَاَلْقِهْ اِلَيْهِمْ ثُمَّ تَوَلَّ عَنْهُمْ فَانْظُرْ مَاذَا يَرْجِعُوْنَ ﴿٢٨﴾

29. Nenda na barua yangu hii na uwafikishie, kisha uwaache, na utazame watajibu nini

قَالَتْ يٰٓاَيُّهَا الْمَلَؤُا اِنِّيْٓ اُلْقِيَ اِلَيَّ كِتٰبٌ كَرِيْمٌ ﴿٢٩﴾

30. (Malkia) akasema: Enyi wakuu (wa baraza)! Hakika nimeletewa barua tukufu:

اِنَّهٗ مِنْ سُلَيْمٰنَ وَاِنَّهٗ بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ ﴿٣٠﴾ۙ

31. Hakika imetoka kwa Suleimani, nayo ni: Kwa jina la Allah, Mwingi wa rehema, Mwingi wa ukarimu.

اَلَّا تَعْلُوْا عَلَيَّ وَاْتُوْنِيْ مُسْلِمِيْنَ ﴿٣١﴾ ع

32. Kwamba msinifanyie jeuri, na fikeni kwangu mkitii.

FUNGU 3

قَالَتْ يٰٓاَيُّهَا الْمَلَؤُا اَفْتُوْنِيْ فِيْٓ اَمْرِيْ ۚ مَا كُنْتُ قَاطِعَةً اَمْرًا حَتّٰى تَشْهَدُوْنِ ﴿٣٣﴾

33. (Malkia) akasema: Enyi wakuu, nipeni shauri katika jambo langu, maana sikati shauri lo lote mpaka mhudhurie.

قَالُوْا نَحْنُ اُولُوْا قُوَّةٍ وَّاُولُوْا بَاْسٍ شَدِيْدٍ ۙ وَّالْاَمْرُ اِلَيْكِ فَانْظُرِيْ مَاذَا تَاْمُرِيْنَ ﴿٣٤﴾

34. Wakasema: Sisi ni wenye nguvu na ni wenye vita kali, na hukumu ni yako, basi utazame ni nini unaamrisha.

قَالَتْ اِنَّ الْمُلُوْكَ اِذَا دَخَلُوْا قَرْيَةً اَفْسَدُوْهَا وَجَعَلُوْٓا اَعِزَّةَ اَهْلِهَآ اَذِلَّةً ۚ وَكَذٰلِكَ يَفْعَلُوْنَ ﴿٣٥﴾

35. (Malkia) akasema: Hakika wafalme wanapouingia mji, wanauharibu na wanawafanya watukufu wake kuwa dhalili; hivi ndivyo wanavyofanya.

وَاِنِّيْ مُرْسِلَةٌ اِلَيْهِمْ بِهَدِيَّةٍ فَنٰظِرَةٌۢ بِمَ يَرْجِعُ الْمُرْسَلُوْنَ ﴿٣٦﴾

36. Na mimi ninawapelekea zawadi, nami nitangoja watakayorudi nayo wajumbe.

فَلَمَّا جَآءَ سُلَيْمٰنَ قَالَ اَتُمِدُّوْنَنِ بِمَالٍ ۖ فَمَآ اٰتٰىنِيَ اللّٰهُ خَيْرٌ مِّمَّآ اٰتٰىكُمْ ۚ بَلْ اَنْتُمْ بِهَدِيَّتِكُمْ تَفْرَحُوْنَ ﴿٣٧﴾

37. Basi alipofika (mjumbe) kwa Suleimani, (Suleimani) akasema: Je, ninyi mnanisaidia kwa mali? Wakati aliyonipa Allah ni bora kuliko Aliyowapeni. Bali ninyi mnajivunia zawadi yenu.

اِرْجِعْ اِلَيْهِمْ فَلَنَاْتِيَنَّهُمْ بِجُنُوْدٍ لَّا قِبَلَ لَهُمْ بِهَا وَلَنُخْرِجَنَّهُمْ مِّنْهَآ اَذِلَّةً وَّهُمْ صٰغِرُوْنَ ﴿٣٨﴾

38. Rudi kwao, kwa yakini tutawafikia na majeshi wasiyoweza kuyakabili, na bila shaka tutawafukuza humo wakidhalilika hali wamekuwa wanyonge.

قَالَ يٰٓاَيُّهَا الْمَلَؤُا اَيُّكُمْ يَاْتِيْنِيْ بِعَرْشِهَا قَبْلَ اَنْ يَّاْتُوْنِيْ مُسْلِمِيْنَ ﴿٣٩﴾

39. Akasema, "Enyi wakuu, ni nani miongoni mwenu atakayenileta kiti chake cha enzi kabla hawajafika kwangu wakitii?

Aya 39. Kutokana na aya zinazofuatia, inabainika kwamba Suleimani hamaanishi kiti cha enzi halisi cha Malkia. Imma ana maana kwamba kiti cha enzi kinachofanana na kile cha Malkia ni lazima kitengenezwe, au kwamba nakala halisi ya kiti cha enzi cha Malkia lazima ipelekwe kwake. Kabla ya ziara yake iliyokusudiwa kwenye mahakama ya Suleimani, Malkia anapata mshangao wa kuona kiti cha enzi kinachofanana sana na kile chake kikiwa katika milki ya Suleimani. Kurtokana na aya zinazofuatia tukio linalojitokeza wazi wazi linaonyesha kwamba kila mmoja miongoni mwa Wazee wa mahakama yake alitaka kazi hiyo apewe yeye, huku kila mmoja akijigamba kwamba ataifanya kazi hiyo haraka sana kuliko washindani wenzake. Hatimaye alipokabidhiwa ile nakala, akamtukuza Allah kwa ajili ya kupatikana kwa nakala

قَالَ عِفْرِيْتٌ مِّنَ الْجِنِّ اَنَا اٰتِيْكَ بِهٖ قَبْلَ اَنْ تَقُوْمَ مِنْ مَّقَامِكَ ۚ وَ اِنِّيْ عَلَيْهِ لَقَوِيٌّ اَمِيْنٌ ﴿٣٩﴾

40. Miongoni mwa majini, Ifriti akasema: Mimi nitakuleteacho kabla hujaondoka mahali hapo umepopafanya kituo, na mimi bila shaka ninazo nguvu za hayo, (na) ni mwaminifu.

قَالَ الَّذِيْ عِنْدَهٗ عِلْمٌ مِّنَ الْكِتٰبِ اَنَا اٰتِيْكَ بِهٖ قَبْلَ اَنْ يَّرْتَدَّ اِلَيْكَ طَرْفُكَ ؕ فَلَمَّا رَاٰهُ مُسْتَقِرًّا عِنْدَهٗ قَالَ هٰذَا مِنْ فَضْلِ رَبِّيْ ۫ لِيَبْلُوَنِيْٓ ءَاَشْكُرُ اَمْ اَكْفُرُ ؕ وَمَنْ شَكَرَ فَاِنَّمَا يَشْكُرُ لِنَفْسِهٖ ۚ وَمَنْ كَفَرَ فَاِنَّ رَبِّيْ غَنِيٌّ كَرِيْمٌ ﴿٤٠﴾

41. Akasema yule aliyekuwa na elimu ya Kitabu: Mimi nitakileta kwa haraka zaidi kuliko kupapasa kwa jicho lako. Na alipokiona kimewekwa mbele yake akasema: Haya yanatokana na fadhili za Mola wangu ili Anijaribu iwapo nitashukuru au nitakufuru? Na anayeshukuru, basi anashukuru kwa ajili ya nafsi yake tu; na anayekufuru, kwa hakika Mola wangu ni Mkwasi, Mkarimu.

قَالَ نَكِّرُوْا لَهَا عَرْشَهَا نَنْظُرْ اَتَهْتَدِيْٓ اَمْ تَكُوْنُ مِنَ الَّذِيْنَ لَا يَهْتَدُوْنَ ﴿٤١﴾

42. (Suleimani) akasema: Kifanye kiti chake cha enzi kionekane kama ni cha kawaida; tutaona kama ataongoka au atakuwa miongoni mwa wale wasioongoka.

فَلَمَّا جَآءَتْ قِيْلَ اَهٰكَذَا عَرْشُكِ ؕ قَالَتْ كَاَنَّهٗ هُوَ ۚ وَاُوْتِيْنَا الْعِلْمَ مِنْ قَبْلِهَا وَكُنَّا مُسْلِمِيْنَ ﴿٤٢﴾

43. Basi (malkia) alipofika akaambiwa: Je, ni kama hiki kiti chako cha enzi? Akasema: Kama ndicho hasa, nasi tulipewa elimu kabla yake na tulishakuwa wenye kutii.

---

hiyo na katoa maagizo ya kuiboresha zaidi ili ifanane kwa karibu zaidi na kile kiti cha enzi cha Malkia wa Sheba ili kupunguza maringo yake ya kuwa na kiti cha enzi cha pekee. Maneno *Nakkiruu lahaa 'arshahaa* yanaunga mkono waziwazi maana hii na yanaashiria kwamba kama tungaliona kiti cha enzi kinachofanana sana na chake, ni dhahiri kwamba ingelimuingia akilini mwake kwamba kiti cha enzi chake mwenyewe si cha pekee na si maalumu kama alivyofikiria. Kwa hiyo maana ya *nakkaruu* kwa maana hii itakifanya kiti chake cha enzi kionekane kuwa ni cha kawaida kiwezacho kuonekana na kila mtu. Alipokiona kidhahiri kiti cha enzi kilichotengenezwa na mafundi wa Suleiman, mwitikio wake haukuwa ule wa Malkia ambaye hivi karibuni tu aliibiwa kiti chake cha enzi, wala ule wa Malkia ambaye hakuweza kutambua kiti cha enzi chake mwenyewe kwa sababu mafundi walikikarabati na kukifanya kisiweze kutambulika. Mwitikio wake ni ule tu wa mtu anayeona kitu kinachofanana na chake. Hii inathibitisha waziwazi kwamba mpangilio wa tukio kwa jinsi tulivyouanisha sisi ndio unaokubalika.

وَصَدَّهَا مَا كَانَتْ تَّعْبُدُ مِنْ دُوْنِ اللّٰهِ ؕ اِنَّهَا كَانَتْ مِنْ قَوْمٍ كٰفِرِيْنَ ﴿٤٤﴾

44. Na (Suleimani) akamkataza yale aliyokuwa akiabudu kinyume cha Allah; bila shaka (malkia huyo) alikuwa katika watu makafiri.

قِيْلَ لَهَا ادْخُلِي الصَّرْحَ ۚ فَلَمَّا رَاَتْهُ حَسِبَتْهُ لُجَّةً وَّكَشَفَتْ عَنْ سَاقَيْهَا ؕ قَالَ اِنَّهٗ صَرْحٌ مُّمَرَّدٌ مِّنْ قَوَارِيْرَ ؕ قَالَتْ رَبِّ اِنِّيْ ظَلَمْتُ نَفْسِيْ وَاَسْلَمْتُ مَعَ سُلَيْمٰنَ لِلّٰهِ رَبِّ الْعٰلَمِيْنَ ﴿٤٤﴾ ع

45. Akaambiwa: Liingie jumba. Lakini alipoliona, akalidhani kuwa ni eneo la maji marefu, na akapandisha nguo kwenye miundi yake. (Suleimani) akasema: Hakika hilo ni jumba lililosakafiwa kwa vioo! Akasema (malkia): Mola wangu, hakika nimedhulumu nafsi yangu, nami najisalimisha pamoja na Suleimani kwa Mola wa walimwengu.

FUNGU 4

وَلَقَدْ اَرْسَلْنَاۤ اِلٰى ثَمُوْدَ اَخَاهُمْ صٰلِحًا اَنِ اعْبُدُوا اللّٰهَ فَاِذَا هُمْ فَرِيْقٰنِ يَخْتَصِمُوْنَ ﴿٤٥﴾

46. Na bila shaka tuliwapelekea Wathamudi ndugu yao Saleh, kuwaambia: mwabuduni Allah. Basi mara wakawa makundi mawili wakigombana.

قَالَ يٰقَوْمِ لِمَ تَسْتَعْجِلُوْنَ بِالسَّيِّئَةِ قَبْلَ الْحَسَنَةِ ۚ لَوْلَا تَسْتَغْفِرُوْنَ اللّٰهَ لَعَلَّكُمْ تُرْحَمُوْنَ ﴿٤٦﴾

47. Akasema Enyi watu wangu! Kwa nini mnaharakia kwenye ubaya kabla ya wema? mbona hamwombi msamaha kwa Allah ili mrehemiwe?

قَالُوا اطَّيَّرْنَا بِكَ وَبِمَنْ مَّعَكَ ؕ قَالَ طٰٓئِرُكُمْ عِنْدَ اللّٰهِ بَلْ اَنْتُمْ قَوْمٌ تُفْتَنُوْنَ ﴿٤٧﴾

48. Wakasema: Tumepata mkosi kwa sababu yako na kwa sababu ya wale walio pamoja nawe. Akasema: mkosi wenu uko kwa Allah. Bali ninyi ni watu mtakaojaribiwa.

Aya 45. *Kashafat'an saaqaihaa*. Maneno haya tumeyatafasiri neno kwa neno, *akapandisha nguo miundi yake*. Lakini kwa desturi maneno haya hutumika katika methali za Kiarabu kuonyesha kuwa mtu alipata wasiwasi na mahangaiko moyoni mwake.

Vioo safi, vyenye ubora wa hali ya juu, vikibandikwa kwa ustadi vyaweza kutengeneza taswira ya maji na hivyo ndivyo hasa ilivyotokea. Ujumbe uliowasilishwa kwa Malkia ambaye alikuwa mwenye akili kupindukia ulikuwa ni huu ya kwamba mara nyingine vitu vinakuwa tofauti sana na taswira zinazotengenezwa na vitu hivyo, na sifa zinazoakisiwa navyo si za vitu hivyo. Kadhalika, taswira ya utukufu wa nguvu zinazoumbwa na jua si za jua bali ni za Mwumbaji tu.

وَكَانَ فِي الْمَدِيْنَةِ تِسْعَةُ رَهْطٍ يُّفْسِدُوْنَ فِي الْاَرْضِ وَلَا يُصْلِحُوْنَ ﴿٤٩﴾

49. Na walikuwamo katika mji wao mkuu watu tisa wakifanya ufisadi katika ardhi wala hawakusuluhisha.

قَالُوْا تَقَاسَمُوْا بِاللّٰهِ لَنُبَيِّتَنَّهٗ وَاَهْلَهٗ ثُمَّ لَنَقُوْلَنَّ لِوَلِيِّهٖ مَا شَهِدْنَا مَهْلِكَ اَهْلِهٖ وَاِنَّا لَصٰدِقُوْنَ ﴿٥٠﴾

50. Wakasema: Apianeni kwa Allah (ya kwamba) tutamshambulia usiku yeye na ahali zake, kisha kwa yakini tutamwambia msimamizi wake: sisi hatukuona maangamio ya ahali zake, na bila shaka sisi ni wakweli.

وَمَكَرُوْا مَكْرًا وَّمَكَرْنَا مَكْرًا وَّهُمْ لَا يَشْعُرُوْنَ ﴿٥١﴾

51. Na wakatunga hila, nasi pia Tukatunga hila, hali hawatambui.

فَانْظُرْ كَيْفَ كَانَ عَاقِبَةُ مَكْرِهِمْ ۙ اَنَّا دَمَّرْنٰهُمْ وَقَوْمَهُمْ اَجْمَعِيْنَ ﴿٥٢﴾

52. Basi angalia ulivyokuwa mwisho wa hila zao, hakika tuliwaangamiza pamoja na watu wao wote.

فَتِلْكَ بُيُوْتُهُمْ خَاوِيَةً ۢ بِمَا ظَلَمُوْا ؕ اِنَّ فِيْ ذٰلِكَ لَاٰيَةً لِّقَوْمٍ يَّعْلَمُوْنَ ﴿٥٣﴾

53. Na huko zimesimama nyumba zao zikiwa tupu, kwa sababu walidhulumu. Bila shaka katika hayo imo ishara kwa watu wanaojua.

وَاَنْجَيْنَا الَّذِيْنَ اٰمَنُوْا وَكَانُوْا يَتَّقُوْنَ ﴿٥٤﴾

54. Na Tukawaokoa wale walioamini na waliokuwa wakimcha (Mungu).

وَلُوْطًا اِذْ قَالَ لِقَوْمِهٖۤ اَتَاْتُوْنَ الْفَاحِشَةَ وَاَنْتُمْ تُبْصِرُوْنَ ﴿٥٥﴾

55. Na Luti alipowaambia watu wake: Je mnaufanya ubaya na hali mnaona?

اَئِنَّكُمْ لَتَاْتُوْنَ الرِّجَالَ شَهْوَةً مِّنْ دُوْنِ النِّسَآءِ ؕ بَلْ اَنْتُمْ قَوْمٌ تَجْهَلُوْنَ ﴿٥٦﴾

56. Nini! Je ninyi mnawaingilia wanaume kwa kutimiza tamaa zenu badala ya wanawake? Bali ninyi ni watu majahili.

Aya 49. *Arrahtu,* "watu," pia lina maana ya *adui* (Munjid). Habari iliyoelezwa hapa ni ya maadui wa Mtume *s.a.w.* ambao wakubwa walikuwa ni watu tisa, nao ni Abu Jahal, Mut'im bin Adiyy, Shaiba bin Rabi'a, 'Utba bin Rabi'a, Walid bin 'Utba, Umayya bin Khalf, Nadhar bin Al-Harith, 'Akba bin Abi Mu'ait na Abu Lahab.

فَمَا كَانَ جَوَابَ قَوْمِهٖٓ اِلَّآ اَنْ قَالُوْٓا اَخْرِجُوْٓا اٰلَ لُوْطٍ مِّنْ قَرْيَتِكُمْ ۚ اِنَّهُمْ اُنَاسٌ يَّتَطَهَّرُوْنَ ﴿٥٦﴾

57. Bali halikuwa jawabu la watu wake isipokuwa kusema: Wafukuzeni wafuasi wa Luti katika mji wenu, hakika hao ni watu wanaojifanya kuwa ni watakatifu.

فَاَنْجَيْنٰهُ وَاَهْلَهٗٓ اِلَّا امْرَاَتَهٗ ۖ قَدَّرْنٰهَا مِنَ الْغٰبِرِيْنَ ﴿٥٧﴾

58. Basi Tulimwokoa yeye na wafuasi wake ila mkewe; Tukamkadiria katika wakaao nyuma.

وَاَمْطَرْنَا عَلَيْهِمْ مَّطَرًا ۚ فَسَآءَ مَطَرُ الْمُنْذَرِيْنَ ﴿٥٨﴾ ع ١٤

59. Na Tukawanyeshelezea mvua; na ilikuwa mbaya namna gani mvua ya wale walioonywa!

FUNGU 5

قُلِ الْحَمْدُ لِلّٰهِ وَسَلٰمٌ عَلٰى عِبَادِهِ الَّذِيْنَ اصْطَفٰى ۭ آٰللّٰهُ خَيْرٌ اَمَّا يُشْرِكُوْنَ ﴿٥٩﴾

60. Sema; Sifa zote njema ni za Allah, na amani iwaendee Watumishi Wake ambao Aliwachagua. Je Allah ni Mbora au wanaowashirikisha?

JUZU 20

اَمَّنْ خَلَقَ السَّمٰوٰتِ وَالْاَرْضَ وَاَنْزَلَ لَكُمْ مِّنَ السَّمَآءِ مَآءً ۚ فَاَنْۢبَتْنَا بِهٖ حَدَآئِقَ ذَاتَ بَهْجَةٍ ۚ مَا كَانَ لَكُمْ اَنْ تُنْۢبِتُوْا شَجَرَهَا ۭ ءَاِلٰهٌ مَّعَ اللّٰهِ ۭ بَلْ هُمْ قَوْمٌ يَّعْدِلُوْنَ ﴿٦٠﴾

61. Au ni nani Aliyeziumba mbingu na ardhi, na Akawateremshieni maji kutoka mawinguni; basi kwayo Tukaziotesha bustani zenye uzuri? Nanyi hamna uwezo wa kuiotesha miti yake. Je, yuko mungu pamoja na Allah? Bali hao ni watu wanaomshirikisha.

اَمَّنْ جَعَلَ الْاَرْضَ قَرَارًا وَّجَعَلَ خِلٰلَهَآ اَنْهٰرًا وَّجَعَلَ لَهَا رَوَاسِيَ وَجَعَلَ بَيْنَ الْبَحْرَيْنِ حَاجِزًا ۭ ءَاِلٰهٌ مَّعَ اللّٰهِ ۭ بَلْ اَكْثَرُهُمْ لَا يَعْلَمُوْنَ ﴿٦١﴾

62. Au ni nani Aliyeifanya ardhi kuwa mahali pa kustarehe, na Akaweka ndani yake mito na Akaiwekea milima, na Akaweka kizuio kati ya bahari mbili? Je, yuko mungu pamoja na Allah? Bali wengi wao hawajui.

اَمَّنْ يُّجِيْبُ الْمُضْطَرَّ اِذَا دَعَاهُ وَيَكْشِفُ السُّوْۗءَ وَيَجْعَلُكُمْ خُلَفَاۗءَ الْاَرْضِ ۭ ءَاِلٰهٌ مَّعَ اللّٰهِ ۭ قَلِيْلًا مَّا تَذَكَّرُوْنَ ﴿٦٢﴾

63. Au ni nani Anayemjibu aliyedhikika amwombapo na kuondoa dhiki, na kuwafanyeni waandamizi duniani? Je, yuko mungu pamoja na Allah? Ni nasaha kidogo tu mnazozishika.

64. Au ni Nani Anaye waongozeni katika giza la bara na bahari, na ni Nani Azipelekaye pepo kutoa habari njema kabla ya rehema Zake? Je, yuko mungu pamoja na Allah? Allah Ametukuka juu ya wale wanaowashirikisha.

اَمَّنْ يَّهْدِيْكُمْ فِيْ ظُلُمٰتِ الْبَرِّ وَالْبَحْرِ وَمَنْ يُّرْسِلُ الرِّيٰحَ بُشْرًا بَيْنَ يَدَيْ رَحْمَتِهٖ ؕ ءَاِلٰهٌ مَّعَ اللّٰهِ ؕ تَعٰلَى اللّٰهُ عَمَّا يُشْرِكُوْنَ ﴿٦٤﴾

65. Au ni Nani Anayeanzisha kiumbe kisha Anakirudisha, na ni Nani Anayewaruzukuni kutoka mbinguni na ardhini? Je, yuko Mungu pamoja na Allah? Sema: Leteni dalili zenu ikiwa mnasema kweli.

اَمَّنْ يَّبْدَؤُا الْخَلْقَ ثُمَّ يُعِيْدُهٗ وَمَنْ يَّرْزُقُكُمْ مِّنَ السَّمَآءِ وَالْاَرْضِ ؕ ءَاِلٰهٌ مَّعَ اللّٰهِ ؕ قُلْ هَاتُوْا بُرْهَانَكُمْ اِنْ كُنْتُمْ صٰدِقِيْنَ ﴿٦٥﴾

66. Sema: Hakuna aliyoko katika mbingu na ardhi ajuaye yasiyoonekana ila Allah; nao hawajui ni lini watafufuliwa.

قُلْ لَّا يَعْلَمُ مَنْ فِي السَّمٰوٰتِ وَالْاَرْضِ الْغَيْبَ اِلَّا اللّٰهُ ؕ وَمَا يَشْعُرُوْنَ اَيَّانَ يُبْعَثُوْنَ ﴿٦٦﴾

67. Lakini imekwisha elimu yao juu ya Akhera, bali wao wamo katika shaka nayo, bali wao ni vipofu nayo.

بَلِ ادّٰرَكَ عِلْمُهُمْ فِي الْاٰخِرَةِ ۚ بَلْ هُمْ فِيْ شَكٍّ مِّنْهَا ۚ بَلْ هُمْ مِّنْهَا عَمُوْنَ ﴿٦٧﴾ ع ۸

FUNGU 6

68. Na wale waliokufuru wakasema: Je, tutakapokuwa udongo sisi na baba zetu, je tutatolewa?

وَقَالَ الَّذِيْنَ كَفَرُوْٓا ءَاِذَا كُنَّا تُرٰبًا وَّاٰبَآؤُنَآ اَئِنَّا لَمُخْرَجُوْنَ ﴿٦٨﴾

69. Bila shaka haya tuliahidiwa sisi na baba zetu zamani; haya siyo ila ni visa tu vya watu wa kale.

لَقَدْ وُعِدْنَا هٰذَا نَحْنُ وَاٰبَآؤُنَا مِنْ قَبْلُ ۙ اِنْ هٰذَآ اِلَّآ اَسَاطِيْرُ الْاَوَّلِيْنَ ﴿٦٩﴾

70. Sema: Tembeeni katika ardhi na mwone jinsi ulivyokuwa mwisho wa wakosefu.

قُلْ سِيْرُوْا فِي الْاَرْضِ فَانْظُرُوْا كَيْفَ كَانَ عَاقِبَةُ الْمُجْرِمِيْنَ ﴿٧٠﴾

71. Wala usiwahuzunikie, wala usiwe katika dhiki kwa sababu ya hila wazifanyazo.

وَلَا تَحْزَنْ عَلَيْهِمْ وَلَا تَكُنْ فِيْ ضَيْقٍ مِّمَّا يَمْكُرُوْنَ ﴿٧١﴾

72. Na wanasema: Ahadi hii itatokea lini ikiwa mnasema kweli?

وَيَقُوْلُوْنَ مَتٰى هٰذَا الْوَعْدُ اِنْ كُنْتُمْ صٰدِقِيْنَ ﴿٧٢﴾

قُلْ عَسٰٓى اَنْ يَّكُوْنَ رَدِفَ لَكُمْ بَعْضُ الَّذِيْ تَسْتَعْجِلُوْنَ ﴿٧٣﴾

73. Sema: Yawezekana kwamba sehemu ya (ile adhabu) mnayoiharakishia iko nyuma yenu.

وَاِنَّ رَبَّكَ لَذُوْ فَضْلٍ عَلَى النَّاسِ وَلٰكِنَّ اَكْثَرَهُمْ لَا يَشْكُرُوْنَ ﴿٧٤﴾

74. Na bila shaka Mola wako ni Mwenye fadhili kwa watu, lakini wengi wao hawashukuru.

وَاِنَّ رَبَّكَ لَيَعْلَمُ مَا تُكِنُّ صُدُوْرُهُمْ وَمَا يُعْلِنُوْنَ ﴿٧٥﴾

75. Na kwa yakini Mola wako Anayajua yanayoficha vifua vyao na wanayoyadhihirisha.

وَمَا مِنْ غَآئِبَةٍ فِى السَّمَآءِ وَالْاَرْضِ اِلَّا فِىْ كِتٰبٍ مُّبِيْنٍ ﴿٧٦﴾

76. Na hakuna siri katika mbingu na ardhi ila imo katika Kitabu kibainishacho.

اِنَّ هٰذَا الْقُرْاٰنَ يَقُصُّ عَلٰى بَنِىْٓ اِسْرَآءِيْلَ اَكْثَرَ الَّذِىْ هُمْ فِيْهِ يَخْتَلِفُوْنَ ﴿٧٧﴾

77. Bila shaka Qur'an hii inawaeleza wana wa Israeli mengi ambayo kwayo wanahitilafiana.

وَاِنَّهٗ لَهُدًى وَّ رَحْمَةٌ لِّلْمُؤْمِنِيْنَ ﴿٧٨﴾

78. Na kwa yakini huo ni mwongozo na rehema kwa waaminio.

اِنَّ رَبَّكَ يَقْضِىْ بَيْنَهُمْ بِحُكْمِهٖ ۚ وَهُوَ الْعَزِيْزُ الْعَلِيْمُ ﴿٧٩﴾

79. Hakika Mola wako Atawakatia baina yao hukumu Yake, naye ni Mwenye nguvu, Mjuzi.

فَتَوَكَّلْ عَلَى اللّٰهِ ۭ اِنَّكَ عَلَى الْحَقِّ الْمُبِيْنِ ﴿٨٠﴾

80. Basi tawakali kwa Allah; hakika wewe u juu ya haki iliyo wazi.

اِنَّكَ لَا تُسْمِعُ الْمَوْتٰى وَلَا تُسْمِعُ الصُّمَّ الدُّعَآءَ اِذَا وَلَّوْا مُدْبِرِيْنَ ﴿٨١﴾

81. Basi kwa hakika huwezi kuwasikilizisha wafu wala huwezi kuwasikilizisha viziwi mwito wako, wanapogeuka kurudi nyuma.

وَمَآ اَنْتَ بِهٰدِى الْعُمْىِ عَنْ ضَلٰلَتِهِمْ ۭ اِنْ تُسْمِعُ اِلَّا مَنْ يُّؤْمِنُ بِاٰيٰتِنَا فَهُمْ مُّسْلِمُوْنَ ﴿٨٢﴾

82. Wala huwezi kuwaongoza vipofu katika upotevu wao. Humsikilizishi isipokuwa yule anayeziamini Aya Zetu, basi hao ndio watii.

Aya 73. *Radifa lakum*, "Ni karibu kuwafikieni." Maneno hayo huonyesha kitu kinachofika baada ya mtu kuondoka, yaani, mara Mtume akitoka adhabu itaanza kuwafikia makafiri. Mahali pengine Allah amesema ya kuwa hatawaadhibu makafiri maadamu Mtume yupo pamoja nao (sura 8:34).

Aya 81. Hapa ni dhahiri kabisa ya kuwa kuwasikilizisha wafu na viziwi sio mradi wake watu waliokufa kabisa na waliokuwa hawasikii, bali mradi wake ni wafu wa roho, maana Allah anasema *wanapogeuka kurudi nyuma*. Hivyo basi Nabii ye yote kuwafufua wafu na

وَاِذَا وَقَعَ الْقَوْلُ عَلَيْهِمْ اَخْرَجْنَا لَهُمْ دَآبَّةً مِّنَ الْاَرْضِ تُكَلِّمُهُمْ ۙ اَنَّ النَّاسَ كَانُوْا بِاٰيٰتِنَا لَا يُوْقِنُوْنَ ﴿٨٣﴾

83. Na hukumu itakapotolewa dhidi yao Tutawatolea kiumbe kutoka ardhini ambacho kitawajeruhi kwa sababu watu hawakuziamini Ishara Zetu.

FUNGU 7

وَيَوْمَ نَحْشُرُ مِنْ كُلِّ اُمَّةٍ فَوْجًا مِّمَّنْ يُّكَذِّبُ بِاٰيٰتِنَا فَهُمْ يُوْزَعُوْنَ ﴿٨٤﴾

84. Na siku Tutakapolikusanya, katika kila umati, kundi miongoni mwa wale wanaokadhibisha Aya Zetu, nao watawekwa mafungu mafungu.

حَتّٰٓى اِذَا جَآءُوْ قَالَ اَكَذَّبْتُمْ بِاٰيٰتِيْ وَلَمْ تُحِيْطُوْا بِهَا عِلْمًا اَمَّاذَا كُنْتُمْ تَعْمَلُوْنَ ﴿٨٥﴾

85. Hata watakapofika, Atasema: Je ninyi mlizikadhibisha Ishara Zangu pasipo kuzijua vyema? Au mlikuwa mkifanya nini?

وَوَقَعَ الْقَوْلُ عَلَيْهِمْ بِمَا ظَلَمُوْا فَهُمْ لَا يَنْطِقُوْنَ ﴿٨٦﴾

86. Na itawaangukia hukumu kwa sababu walidhulumu, nao hawatakuwa na uwezo wa kusema.

اَلَمْ يَرَوْا اَنَّا جَعَلْنَا الَّيْلَ لِيَسْكُنُوْا فِيْهِ وَالنَّهَارَ مُبْصِرًا ۭ اِنَّ فِيْ ذٰلِكَ لَاٰيٰتٍ لِّقَوْمٍ يُّؤْمِنُوْنَ ﴿٨٧﴾

87. Je, hawaoni ya kwamba Tumeufanya usiku ili watulie humo, na mchana uangazao? Kwa yakini katika hayo zimo Ishara kwa watu wanaoamini.

وَيَوْمَ يُنْفَخُ فِي الصُّوْرِ فَفَزِعَ مَنْ فِي السَّمٰوٰتِ وَمَنْ فِي الْاَرْضِ اِلَّا مَنْ شَآءَ اللّٰهُ ۭ وَكُلٌّ اَتَوْهُ دٰخِرِيْنَ ﴿٨٨﴾

88. Na siku itakapopulizwa parapanda, ndipo watakapohangaika waliomo mbinguni na waliomo ardhini ila yule Allah Amtakaye, na wote watamfikia wakinyenyekea.

وَتَرَى الْجِبَالَ تَحْسَبُهَا جَامِدَةً وَّهِيَ تَمُرُّ مَرَّ السَّحَابِ ۭ صُنْعَ اللّٰهِ الَّذِيْٓ اَتْقَنَ

89. Na utaona milima ukaidhani kwamba imetuwama hali inapita mpito wa mawingu.

---

kuwaponya vipofu mradi wake hasa ni wafu waliofariki roho, si viwiliwili, na vipofu wa roho.

Aya 83. *Kauli itakapowaangukia,* yaani dalili zote za ukweli watakapoziambiwa na hoja zote kukamilika, nao wasitake kushika haki, hapo watahukumiwa kuwa wakosefu na wataadhibiwa.

Mdudu katika ardhi. Maneno haya yana maana mbili: (1) maulamaa wasio na maarifa ya kimbingu, wenye akili za kidunia tu; (2) vijidudu vya maradhi kama tauni.

Maadui wa Manabii pengine huadhibiwa kwa vijidudu. Na katika hadithi iliyo katika Muslim imeandikwa ya kuwa atakapofika Masihi Aliyeahidiwa maadui zake watajeruhiwa na vijidudu vya tauni.

Aya 89. *Milima.* Watu wakubwa huitwa milima. Katika vita vya Badri wakubwa wote

كُلَّ شَيْءٍ ۭ اِنَّهٗ خَبِيْرٌۢ بِمَا تَفْعَلُوْنَ ۝٨٨

Hiyo ndiyo sanaa ya Allah, Aliyekifanya kila kit kuwa imara na madhubuti. Bila shaka Anayajua vizuri sana yale mnayoyatenda.

مَنْ جَاۗءَ بِالْحَسَنَةِ فَلَهٗ خَيْرٌ مِّنْهَا ۚ وَهُمْ مِّنْ فَزَعٍ يَّوْمَىِٕذٍ اٰمِنُوْنَ ۝٨٩

90. Atakayeleta mema, basi atapata mema kuliko hayo, nao katika mahangaiko ya Siku hiyo watasalimika.

وَمَنْ جَاۗءَ بِالسَّيِّئَةِ فَكُبَّتْ وُجُوْهُهُمْ فِي النَّارِ ۭ هَلْ تُجْزَوْنَ اِلَّا مَا كُنْتُمْ تَعْمَلُوْنَ ۝٩٠

91. Na watakaoleta ubaya, basi zitaangushwa nyuso zao Motoni: Hamtalipwa isipokuwa yale mliyokuwa mkitenda!

اِنَّمَآ اُمِرْتُ اَنْ اَعْبُدَ رَبَّ هٰذِهِ الْبَلْدَةِ الَّذِيْ حَرَّمَهَا وَلَهٗ كُلُّ شَيْءٍ ۡ وَّاُمِرْتُ اَنْ اَكُوْنَ مِنَ الْمُسْلِمِيْنَ ۝٩١ۙ

92. Bila shaka nimeamrishwa nimwabudu Mola wa mji huu Ambaye Ameutakasa; na ni vyake vitu vyote; na nimeamrishwa niwe miongoni mwa wanaonyenyekea.

وَاَنْ اَتْلُوَا الْقُرْاٰنَ ۚ فَمَنِ اهْتَدٰى فَاِنَّمَا يَهْتَدِيْ لِنَفْسِهٖ ۚ وَمَنْ ضَلَّ فَقُلْ اِنَّمَآ اَنَا مِنَ الْمُنْذِرِيْنَ ۝٩٢

93. Na ya kwamba nisome Qur'an. Na mwenye kuongoka, basi ameongoka kwa (faida ya) nafsi yake tu; na aliyepotea, basi sema: Hakika mimi ni miongoni mwa Waonyaji tu.

وَقُلِ الْحَمْدُ لِلّٰهِ سَيُرِيْكُمْ اٰيٰتِهٖ فَتَعْرِفُوْنَهَا ۭ وَمَا رَبُّكَ بِغَافِلٍ عَمَّا تَعْمَلُوْنَ ۝٩٣ۧ

94. Na sema: Sifa zote njema ni za Allah, karibuni Atawaonyesheni Ishara Zake na mtazifahamu; wala Mola wako Haghafiliki na hayo mnayofanya.

---

waliokuwa maadui wa dini ya Kiislamu waliuawa. Kadhalika Aya hii ni bishara juu ya kuvunjika falme kubwa-kubwa za Kisra na Kaisar zilizokuwa kama milima. Waidha milima kupita pia ni jambo ambalo hasa siku hizi limeonekana wazi iliposawazishwa milima kwa mabomu wakati wa vita.

Aya 92. *Mji huu,* yaani mji wa Makka.

Aya 93. *Nisome Qur'an.* Habari zote za kufanikiwa zimo katika Qur'an. Waislamu wa zamani walifanikiwa kwa sababu walifanya bidii kuisoma Qur'an na kufahamu inaagiza nini na wakafuata maagizo yake, basi wakafanikiwa. Na baadaye Waislamu wameanza kuanguka kwa sababu hawakushika maagizo ya Qur'an; na ingawa waliisoma lakini hawakujali inayoyaagiza.

سُوْرَةُ الْقَصَصِ مَكِّيَّةٌ وَّ هِيَ مَعَ الْبَسْمَلَةِ تِسْعٌ وَّ ثَمَانُوْنَ اٰيَةً وَّ تِسْعَةُ رُكُوْعَاتٍ

28. SURA AL-QASAS

Imeteremshwa Makka

Ina mafungu 9 na Aya 89 pamoja na Bismillahi

بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ ①

1. Kwa jina la Allah, Mwingi wa rehema, Mwingi wa ukarimu.

طٰسٓمٓ ②

2. (Allah) Atakasaye, Asikiaye, Ajuaye.

تِلْكَ اٰيٰتُ الْكِتٰبِ الْمُبِيْنِ ③

3. Hizi ni Aya za Kitabu kielezacho.

نَتْلُوْا عَلَيْكَ مِنْ نَّبَاِ مُوْسٰى وَ فِرْعَوْنَ بِالْحَقِّ لِقَوْمٍ يُّؤْمِنُوْنَ ④

4. Tunakusomea habari za Musa na Firauni kwa haki, kwa ajili ya watu wanaoamini

اِنَّ فِرْعَوْنَ عَلَا فِي الْاَرْضِ وَ جَعَلَ اَهْلَهَا شِيَعًا يَّسْتَضْعِفُ طَآئِفَةً مِّنْهُمْ يُذَبِّحُ اَبْنَآءَهُمْ وَ يَسْتَحْيٖ نِسَآءَهُمْ ؕ اِنَّهٗ كَانَ مِنَ الْمُفْسِدِيْنَ ⑤

5. Hakika Firauni aliasi kupita kiasi katika ardhi, na akawatenganisha wenyeji wake katika makundi, akilidhoofisha taifa moja miongoni mwao, kwa kuwachinja watoto wao wa kiume na kuwaacha hai wanawake wao. Hakika yeye alikuwa miongoni mwa waharibifu.

Inasemekana ya kuwa sura hii ilishuka kwa Mtume wakati alipokuwa akihama kutoka Makka kwenda Madina mahali paitwapo Jahfa (Ibni Abbas, Muhit). Wengine wanasema ni Aya 86 tu inayoeleza kurudi Makka kwa Mtume s.a.w. hali ameshinda ndiyo iliyoshuka mahali pale (Ibni Salaam , Muhit), na hii ndiyo inaonekana kuwa sawa.

Aya 2. *Taa Siin Miim.* Hizi ni herufi za mkato za sifa hizi za Allah: *Taa* ni *Taahir* (Anayetakasa), *Siin* ni *Samii'* (Asikiaye), *Miim* ni *'Aliim* (Ajuaye).

Aya 3. *Mubiin* "Kielezacho." neno hili maana yake pia ni "kipambanuacho." Mradi wa Aya hii ni kuwa Qur'an inaeleza na kupambanua baina ya haramu na halali, baina ya haki na uwongo, na pia inapambanua makosa yaliyoingizwa na watu katika Vitabu vya zamani.

Aya 4. Waaminio wanaelezwa katika sura hii habari zilizotokea baina ya Nabii Musa na Firauni ili ziwe mawaidha kwa ajili yao.

Aya 5. *Akawatenganisha wenyeji wake katika makundi.* Ni desturi inayojulikana toka siku nyingi ya kuwa wafalme, kwa kutaka raia wasiunganike juu ya jambo moja, wanawasaliti na kuwafanya makundi makundi ili waweze kuwatawala wapendavyo. Basi haya ni mawaidha kwa ajili ya Waislamu ya kuwa wasifanyiane uadui kwa sababu ya hitilafu ndogo ndogo, bali wadumu kila wakati katika umoja.

6. Na Twataka kuwafanyia hisani wale waliodhoofishwa katika ardhi na kuwafanya viongozi, na kuwafanya warithi.

وَنُرِيْدُ اَنْ نَّمُنَّ عَلَى الَّذِيْنَ اسْتُضْعِفُوْا فِى الْاَرْضِ وَنَجْعَلَهُمْ اَئِمَّةً وَّنَجْعَلَهُمُ الْوٰرِثِيْنَ ۙ﴿٦﴾

7. Na kuwapa nguvu ardhini; na kuwaonyesha katika hao Firauni na Hamana na majeshi yao yale waliyokuwa wakiyaogopa.

وَنُمَكِّنَ لَهُمْ فِى الْاَرْضِ وَنُرِىَ فِرْعَوْنَ وَهَامٰنَ وَجُنُوْدَهُمَا مِنْهُمْ مَّا كَانُوْا يَحْذَرُوْنَ ﴿٧﴾

8. Na Tulimfunulia mama wa Musa ya kwamba mnyonyeshe, na utakapomhofia, basi mtie mtoni, na usiogope wala usihuzunike, kwa hakika sisi Tutamrudisha kwako, na Tutamfanya miongoni mwa Mitume.

وَاَوْحَيْنَآ اِلٰٓى اُمِّ مُوْسٰٓى اَنْ اَرْضِعِيْهِ ۚ فَاِذَا خِفْتِ عَلَيْهِ فَاَلْقِيْهِ فِى الْيَمِّ وَلَا تَخَافِىْ وَلَا تَحْزَنِىْ ۚ اِنَّا رَآدُّوْهُ اِلَيْكِ وَجَاعِلُوْهُ مِنَ الْمُرْسَلِيْنَ ﴿٨﴾

9. Na wakamuokota watu wa Firauni awe kwao adui na sababu ya huzuni. Bila shaka Firauni na Hamana na majeshi yao walikuwa wenye hatia.

فَالْتَقَطَهٗٓ اٰلُ فِرْعَوْنَ لِيَكُوْنَ لَهُمْ عَدُوًّا وَّحَزَنًا ؕ اِنَّ فِرْعَوْنَ وَهَامٰنَ وَجُنُوْدَهُمَا كَانُوْا خٰطِـِٕيْنَ ﴿٩﴾

10. Na mkewe Firauni akasema: Kiburudisho cha macho kwangu na kwako; msimwue, huenda atatunufaisha, au tutampanga kuwa mwana, hali hawatambui.

وَقَالَتِ امْرَاَتُ فِرْعَوْنَ قُرَّتُ عَيْنٍ لِّىْ وَلَكَ ؕ لَا تَقْتُلُوْهُ ۖ عَسٰٓى اَنْ يَّنْفَعَنَآ اَوْ نَتَّخِذَهٗ وَلَدًا وَّهُمْ لَا يَشْعُرُوْنَ ﴿١٠﴾

11. Na wasiwasi ukatoweka katika moyo wa mama yake Musa. Alikuwa karibu kudhihirisha utambulisho wake (Musa) kama Tusingalimuimarisha moyo wake ili awe miongoni mwa waaminio.

وَاَصْبَحَ فُؤَادُ اُمِّ مُوْسٰى فٰرِغًا ؕ اِنْ كَادَتْ لَتُبْدِىْ بِهٖ لَوْلَآ اَنْ رَّبَطْنَا عَلٰى قَلْبِهَا لِتَكُوْنَ مِنَ الْمُؤْمِنِيْنَ ﴿١١﴾

12. Na akamwambia dada yake (Musa): Mfuate. Basi yeye akamwangalia kwa mbali bila wao kujua.

وَقَالَتْ لِاُخْتِهٖ قُصِّيْهِ ۖ فَبَصُرَتْ بِهٖ عَنْ جُنُبٍ وَّهُمْ لَا يَشْعُرُوْنَ ۙ﴿١٢﴾

Aya 6. Hapa Allah anawajulisha wale wanaodhoofishwa ya kuwa Yeye Mwenyewe hutaka kuwafanyia hisani na kuwainua kuwa viongozi.

13. Na Tukamharamishia wanyonyeshaji tangu mwanzo; kwa hiyo (dada yake) akasema: Je niwaonyesheni watu wa nyumba ambao watamlea kwa ajili yenu na pia watakuwa wema kwake?

وَحَرَّمْنَا عَلَيْهِ الْمَرَاضِعَ مِنْ قَبْلُ فَقَالَتْ هَلْ اَدُلُّكُمْ عَلٰٓى اَهْلِ بَيْتٍ يَّكْفُلُوْنَهٗ لَكُمْ وَهُمْ لَهٗ نٰصِحُوْنَ ﴿١٣﴾

14. Basi Tukamrudisha kwa mama yake ili macho yake yaburudike, wala asihuzunike na ajue ya kwamba ahadi ya Allah ni kweli, lakini wengi wao hawajui.

فَرَدَدْنٰهُ اِلٰٓى اُمِّهٖ كَيْ تَقَرَّ عَيْنُهَا وَلَا تَحْزَنَ وَلِتَعْلَمَ اَنَّ وَعْدَ اللّٰهِ حَقٌّ وَّلٰكِنَّ اَكْثَرَهُمْ لَا يَعْلَمُوْنَ ﴿١٤﴾ ع

FUNGU 2

15. Na (Musa) alipofika balehe yake na akakomaa, Tukampa hukumu na elimu na hivi ndivyo Tuwalipavyo wafanyao wema.

وَلَمَّا بَلَغَ اَشُدَّهٗ وَاسْتَوٰٓى اٰتَيْنٰهُ حُكْمًا وَّعِلْمًا ؕ وَكَذٰلِكَ نَجْزِى الْمُحْسِنِيْنَ ﴿١٥﴾

16. Na aliingia mjini wakati wenyeji wake walikuwa wameghafilika, na akakuta humo watu wawili wakipigana: huyu wa jamii yake na huyu wa adui zake. Basi yule wa jamii yake akamuomba msaada dhidi ya yule wa adui yake. Ndipo Musa akampiga ngumi, na akammaliza. Akasema: Hiki ni kitendo cha Shetani; bila shaka yeye ni adui, mpotezaji dhahiri.

وَدَخَلَ الْمَدِيْنَةَ عَلٰى حِيْنِ غَفْلَةٍ مِّنْ اَهْلِهَا فَوَجَدَ فِيْهَا رَجُلَيْنِ يَقْتَتِلٰنِ ۚ هٰذَا مِنْ شِيْعَتِهٖ وَهٰذَا مِنْ عَدُوِّهٖ ۚ فَاسْتَغَاثَهُ الَّذِىْ مِنْ شِيْعَتِهٖ عَلَى الَّذِىْ مِنْ عَدُوِّهٖ ۙ فَوَكَزَهٗ مُوْسٰى فَقَضٰى عَلَيْهِ ۚ قَالَ هٰذَا مِنْ عَمَلِ الشَّيْطٰنِ ؕ اِنَّهٗ عَدُوٌّ مُّضِلٌّ مُّبِيْنٌ ﴿١٦﴾

17. Akasema: Mola wangu! Bila shaka nimeidhulumu nafsi yangu, basi Unisamehe; naye Akamsamehe. Kwa yakini Yeye ni Msamehevu, Mrehemevu.

قَالَ رَبِّ اِنِّىْ ظَلَمْتُ نَفْسِىْ فَاغْفِرْ لِىْ فَغَفَرَ لَهٗ ؕ اِنَّهٗ هُوَ الْغَفُوْرُ الرَّحِيْمُ ﴿١٧﴾

Aya 16. *Hiki ni kitendo cha shetani;* yaani yule adui alipewa adhabu ile ya kupigwa kwa sababu ya tendo la kishetani alilomfanyia mwenziwe.

Aya 17. *Nimedhulumu nafsi yangu;* yaani sikukusudia kumwua mtu huyu, lakini amekufa na matata yatatokea na bila shaka nitaingia taabuni. *Neno ghofira tulilofasiri kusamehe,* kwa Kiarabu lina maana ya kufunika na kusitiri pia. Basi Nabii Musa aliomba amsitiri na ayafunike matata yasitokee kwa ajili ya kufa mtu yule, na Mungu akamsitiri.

قَالَ رَبِّ بِمَآ اَنْعَمْتَ عَلَيَّ فَلَنْ اَكُوْنَ ظَهِيْرًا لِّلْمُجْرِمِيْنَ ﴿١٨﴾

18. Akasema: Mola wangu, kwa sababu uumenineemesha, basi sitakuwa kabisa msaidizi wa wakosefu.

فَاَصْبَحَ فِي الْمَدِيْنَةِ خَآئِفًا يَّتَرَقَّبُ فَاِذَا الَّذِي اسْتَنْصَرَهٗ بِالْاَمْسِ يَسْتَصْرِخُهٗ ؕ قَالَ لَهٗ مُوْسٰٓى اِنَّكَ لَغَوِيٌّ مُّبِيْنٌ ﴿١٩﴾

19. Na alikwenda mjini asubuhi kwa tahadhari akiogopa; mara yule mtu aliyemwomba msaada jana alimwita tena ili amsaidie. Musa akamwambia bila shaka wewe ni mkosaji dhahiri.

فَلَمَّآ اَنْ اَرَادَ اَنْ يَّبْطِشَ بِالَّذِيْ هُوَ عَدُوٌّ لَّهُمَا ۙ قَالَ يٰمُوْسٰٓى اَتُرِيْدُ اَنْ تَقْتُلَنِيْ كَمَا قَتَلْتَ نَفْسًۢا بِالْاَمْسِ ۖ اِنْ تُرِيْدُ اِلَّآ اَنْ تَكُوْنَ جَبَّارًا فِي الْاَرْضِ وَمَا تُرِيْدُ اَنْ تَكُوْنَ مِنَ الْمُصْلِحِيْنَ ﴿٢٠﴾

20. Basi alipotaka kumkamata yeye aliye adui yao wote wawili, akasema: Ewe Musa, je, unataka kuniua kama ulivyomuua mtu jana? Wewe hutaki ila kuwa jabari katika nchi wala hutaki kuwa miongoni mwa wasuluhishi.

وَجَآءَ رَجُلٌ مِّنْ اَقْصَا الْمَدِيْنَةِ يَسْعٰى ۫ قَالَ يٰمُوْسٰٓى اِنَّ الْمَلَاَ يَاْتَمِرُوْنَ بِكَ لِيَقْتُلُوْكَ فَاخْرُجْ اِنِّيْ لَكَ مِنَ النّٰصِحِيْنَ ﴿٢١﴾

21. Na akaja mtu kutoka mwisho wa mji akikimbia, akasema: Ewe Musa! hakika wakubwa wanashauriana kukuua, basi uondoke; bila shaka mimi ni miongoni mwa wakutakiao wema.

فَخَرَجَ مِنْهَا خَآئِفًا يَّتَرَقَّبُ ۫ قَالَ رَبِّ نَجِّنِيْ مِنَ الْقَوْمِ الظّٰلِمِيْنَ ﴿٢٢﴾ ع ٢

22. Basi (Musa) akaondoka kwa tahadhari akiogopa, (na) akasema: Mola wangu, niokoe katika watu wadhalimu.

FUNGU 3

وَلَمَّا تَوَجَّهَ تِلْقَآءَ مَدْيَنَ قَالَ عَسٰى رَبِّيْٓ اَنْ يَّهْدِيَنِيْ سَوَآءَ السَّبِيْلِ ﴿٢٣﴾

23. Na alipoelekea upande wa Madiani, akasema: Asaa Mola wangu Ataniongoza njia iliyo sawa.

وَلَمَّا وَرَدَ مَآءَ مَدْيَنَ وَجَدَ عَلَيْهِ اُمَّةً مِّنَ النَّاسِ يَسْقُوْنَ ۖ وَوَجَدَ مِنْ دُوْنِهِمُ امْرَاَتَيْنِ تَذُوْدٰنِ ۚ قَالَ مَا خَطْبُكُمَا ؕ قَالَتَا لَا نَسْقِيْ حَتّٰى يُصْدِرَ الرِّعَآءُ ؕ وَاَبُوْنَا شَيْخٌ كَبِيْرٌ ﴿٢٤﴾

24. Na alipoyafikia maji ya Madiani akakuta kundi la watu wakinywesha, na akakuta nyuma yao wanawake wawili wakiwazuia (wanyama wao), akasema: Mna haja gani? Wote wawili wakasema: Hatunyweshi mpaka wachungaji warudishe (wanyama wao), na baba yetu ni mzee sana.

Aya 18. Hapa Nabii Musa anatoa shukurani Kwa Allah ya kuwa amemneemesha kwa sababu alimsaidia mtu aliyedhulumiwa, na sasa kila siku atawasaidia wanaodhulumiwa na hatawasaidia wakosefu.

فَسَقٰى لَهُمَا ثُمَّ تَوَلّٰٓى اِلَى الظِّلِّ فَقَالَ
رَبِّ اِنِّىْ لِمَآ اَنْزَلْتَ اِلَىَّ مِنْ خَيْرٍ فَقِيْرٌ ﴿٢٥﴾

25. Basi (Musa) akawanyweshea wanyama wao. Kisha akarudi kivulini na kusema: Ewe Mola wangu, mimi ni mhitaji wa heri yo yote Utakayoniteremshia.

فَجَآءَتْهُ اِحْدٰىهُمَا تَمْشِىْ عَلَى اسْتِحْيَآءٍ ۖ
قَالَتْ اِنَّ اَبِىْ يَدْعُوْكَ لِيَجْزِيَكَ اَجْرَ
مَا سَقَيْتَ لَنَا ۭ فَلَمَّا جَآءَهٗ وَقَصَّ
عَلَيْهِ الْقَصَصَ ۙ قَالَ لَا تَخَفْ ۡ
نَجَوْتَ مِنَ الْقَوْمِ الظّٰلِمِيْنَ ﴿٢٦﴾

26. Basi akamjia mmoja katika wale wawili akitembea kwa haya, akasema: Baba yangu anakuita ili akulipe ujira wa kutunyweshea. Basi alipomfikia na akamsimulia kisa chote, akasema: Usiogope, umekwisha okoka katika watu wadhalimu.

قَالَتْ اِحْدٰىهُمَا يٰٓاَبَتِ اسْتَاْجِرْهُ ۖ اِنَّ
خَيْرَ مَنِ اسْتَاْجَرْتَ الْقَوِىُّ الْاَمِيْنُ ﴿٢٧﴾

27. Akasema mmoja wa wale wawili: Ewe baba yangu! mwajiri. Bila shaka mbora uwezaye kumwajiri ni yule mwenye nguvu, mwaminifu.

قَالَ اِنِّىْٓ اُرِيْدُ اَنْ اُنْكِحَكَ اِحْدَى
ابْنَتَىَّ هٰتَيْنِ عَلٰٓى اَنْ تَاْجُرَنِىْ ثَمٰنِىَ حِجَجٍ ۚ
فَاِنْ اَتْمَمْتَ عَشْرًا فَمِنْ عِنْدِكَ ۚ وَمَآ
اُرِيْدُ اَنْ اَشُقَّ عَلَيْكَ ۭ سَتَجِدُنِىْٓ اِنْ شَآءَ
اللّٰهُ مِنَ الصّٰلِحِيْنَ ﴿٢٨﴾

28. Akasema: Mimi nataka nikuoze mmojawapo katika binti zangu hawa kwa kunitumikia miaka minane; na kama ukitimiza kumi ni hiari yako, lakini mimi sitaki kukutaabisha: utanikuta insha-Alllah miongoni mwa watu wema.

قَالَ ذٰلِكَ بَيْنِىْ وَبَيْنَكَ ۭ اَيَّمَا الْاَجَلَيْنِ
قَضَيْتُ فَلَا عُدْوَانَ عَلَىَّ ۭ وَاللّٰهُ عَلٰي مَا
نَقُوْلُ وَكِيْلٌ ﴿٢٩﴾ ع ٣

29. Akasema (Musa: Mapatano) hayo yamekwisha kuwa baina yangu na baina yako; muda mmojapo nitakapomaliza, basi nisidhulumiwe; na Allah ni Shahidi juu ya hayo tunayosema.

FUNGU 4

فَلَمَّا قَضٰى مُوْسَى الْاَجَلَ وَسَارَ بِاَهْلِهٖٓ
اٰنَسَ مِنْ جَانِبِ الطُّوْرِ نَارًا ۚ قَالَ
لِاَهْلِهِ امْكُثُوْٓا اِنِّىْٓ اٰنَسْتُ نَارًا لَّعَلِّىْٓ
اٰتِيْكُمْ مِّنْهَا بِخَبَرٍ اَوْ جَذْوَةٍ مِّنَ النَّارِ
لَعَلَّكُمْ تَصْطَلُوْنَ ﴿٣٠﴾

30. Basi Musa alipotimiza muda, akasafiri pamoja na ahali zake, Akaona moto upande wa mlima. Akawaambia ahali zake: Ngojeni, hakika nimeona moto labda nitawaleteeni habari za huko au kijinga cha moto ili mwote.

Aya 27. *Mwaminifu.* Hapa uaminifu wa Nabii Musa unashuhudiwa na kijana wa kike, ingawa Musa alikuwa bado kijana tu.

فَلَمَّآ اَتٰىهَا نُوْدِيَ مِنْ شَاطِئِ الْوَادِ الْاَيْمَنِ
فِي الْبُقْعَةِ الْمُبٰرَكَةِ مِنَ الشَّجَرَةِ اَنْ
يّٰمُوْسٰٓى اِنِّيْٓ اَنَا اللّٰهُ رَبُّ الْعٰلَمِيْنَ ﴿٣١﴾

31. Basi alipoufikia aliitwa kutoka upande wa kuume wa bonde, katika kiwanja kilichobarikiwa, kutoka mtini, ya kwamba ewe Musa, bila shaka Mimi Ndiye Allah Mola wa walimwengu.

وَاَنْ اَلْقِ عَصَاكَ ؕ فَلَمَّا رَاٰهَا تَهْتَزُّ
كَاَنَّهَا جَآنٌّ وَّلّٰى مُدْبِرًا وَّلَمْ يُعَقِّبْ ؕ
يٰمُوْسٰٓى اَقْبِلْ وَلَا تَخَفْ ۖ اِنَّكَ مِنَ
الْاٰمِنِيْنَ ﴿٣٢﴾

32. Na ya kwamba, tupa fimbo yako. Basi alipoiona ikichezacheza kama nyoka akageuka bila kutazama nyuma. Ewe Musa, njoo mbele na usiogope, kwa yakini wewe u miongoni mwa waliosalimika.

اُسْلُكْ يَدَكَ فِيْ جَيْبِكَ تَخْرُجْ
بَيْضَآءَ مِنْ غَيْرِ سُوْٓءٍ ۫ وَّاضْمُمْ اِلَيْكَ
جَنَاحَكَ مِنَ الرَّهْبِ فَذٰنِكَ بُرْهَانٰنِ مِنْ
رَّبِّكَ اِلٰى فِرْعَوْنَ وَمَلَا۟ئِهٖ ؕ اِنَّهُمْ كَانُوْا
قَوْمًا فٰسِقِيْنَ ﴿٣٣﴾

33. Ingiza mkono wako kifuani mwako utatoka mweupe pasipo maradhi, na uvutie kwako mkono wako kutuliza hofu! Basi hizi zitakuwa dalili mbili zitokazo kwa Mola wako kwa ajili ya Firauni na wakuu wake; bila shaka hao ni watu waasi.

قَالَ رَبِّ اِنِّيْ قَتَلْتُ مِنْهُمْ نَفْسًا
فَاَخَافُ اَنْ يَّقْتُلُوْنِ ﴿٣٤﴾

34. (Musa) akasema: Mola wangu, hakika mimi nilimwua mtu kati yao, kwa hiyo naogopa wataniua.

وَاَخِيْ هٰرُوْنُ هُوَ اَفْصَحُ مِنِّيْ لِسَانًا
فَاَرْسِلْهُ مَعِيَ رِدْاً يُّصَدِّقُنِيْٓ ۫ اِنِّيْٓ
اَخَافُ اَنْ يُّكَذِّبُوْنِ ﴿٣٥﴾

35. Na ndugu yangu Harun ni fasihi zaidi kuliko mimi kwa usemi, basi Umtume pamoja nami awe msaidizi, kunisadikisha; hakika mimi naogopa ya kwamba watanikadhibisha.

قَالَ سَنَشُدُّ عَضُدَكَ بِاَخِيْكَ وَنَجْعَلُ
لَكُمَا سُلْطٰنًا فَلَا يَصِلُوْنَ اِلَيْكُمَا ۚۛ
بِاٰيٰتِنَآ ۚۛ اَنْتُمَا وَمَنِ اتَّبَعَكُمَا الْغٰلِبُوْنَ ﴿٣٦﴾

36. (Allah) Akasema: Karibuni Tutautia nguvu mkono wako kwa kupitia ndugu yako, na Tutawapeni ushindi hata hawatawafikieni - kwa sababu ya Ishara Zetu ninyi na watakaowafuateni mtashinda.

فَلَمَّا جَآءَهُمْ مُّوْسٰى بِاٰيٰتِنَا بَيِّنٰتٍ قَالُوْا
مَا هٰذَآ اِلَّا سِحْرٌ مُّفْتَرًى وَّمَا سَمِعْنَا
بِهٰذَا فِيْٓ اٰبَآئِنَا الْاَوَّلِيْنَ ﴿٣٧﴾

37. Basi alipowafikia Musa na Ishara Zetu waziwazi, wakasema: Huu sio ila ni uchawi uliotungwa, wala hatukuyasikia haya kwa baba zetu wa zamani.

وَقَالَ مُوْسٰى رَبِّيْٓ اَعْلَمُ بِمَنْ جَآءَ بِالْهُدٰى مِنْ عِنْدِهٖ وَمَنْ تَكُوْنُ لَهٗ عَاقِبَةُ الدَّارِ ؕ اِنَّهٗ لَا يُفْلِحُ الظّٰلِمُوْنَ ﴿۳۸﴾

38. Na Musa akasema: Mola wangu ndiye Amjuaye sana yule aliyekuja na mwongozo kutoka Kwake, na nani atakayekuwa na nyumba ya Akhera; hakika wadhalimu hawatafaulu.

وَقَالَ فِرْعَوْنُ يٰٓاَيُّهَا الْمَلَاُ مَا عَلِمْتُ لَكُمْ مِّنْ اِلٰهٍ غَيْرِيْ ۚ فَاَوْقِدْ لِيْ يٰهَامٰنُ عَلَى الطِّيْنِ فَاجْعَلْ لِّيْ صَرْحًا لَّعَلِّيْٓ اَطَّلِعُ اِلٰٓى اِلٰهِ مُوْسٰى ۙ وَاِنِّيْ لَاَظُنُّهٗ مِنَ الْكٰذِبِيْنَ ﴿۳۹﴾

39. Na Firauni akasema: Enyi wakuu! Simjui kwa ajili yenu mungu minghairi yangu. Basi ewe Hamana, niwashie moto juu ya udongo, na unijengee mnara ili nimchungulie Mungu wa Musa, na kwa yakini namdhani kuwa yu katika waongo.

وَاسْتَكْبَرَ هُوَ وَجُنُوْدُهٗ فِي الْاَرْضِ بِغَيْرِ الْحَقِّ وَظَنُّوْٓا اَنَّهُمْ اِلَيْنَا لَا يُرْجَعُوْنَ ﴿۴۰﴾

40. Na alijivuna yeye na majeshi yake katika nchi pasipo haki na walidhani ya kwamba hawatarudishwa Kwetu.

فَاَخَذْنٰهُ وَجُنُوْدَهٗ فَنَبَذْنٰهُمْ فِي الْيَمِّ ۚ فَانْظُرْ كَيْفَ كَانَ عَاقِبَةُ الظّٰلِمِيْنَ ﴿۴۱﴾

41. Basi Tukamshika yeye na majeshi yake na Tukawatupa baharini, basi angalia ulikuwaje mwisho wa wadhalimu.

وَجَعَلْنٰهُمْ اَئِمَّةً يَّدْعُوْنَ اِلَى النَّارِ ۚ وَيَوْمَ الْقِيٰمَةِ لَا يُنْصَرُوْنَ ﴿۴۲﴾

42. Na Tukawafanya viongozi waitao kwenye Moto, na siku ya Kiyama hawatasaidiwa.

وَاَتْبَعْنٰهُمْ فِيْ هٰذِهِ الدُّنْيَا لَعْنَةً ۚ وَيَوْمَ الْقِيٰمَةِ هُمْ مِّنَ الْمَقْبُوْحِيْنَ ﴿۴۳﴾ ع ۷

43. Na Tukawafuatishia laana katika dunia hii, na siku ya Kiyama wao watakuwa miongoni mwa wenye hali mbaya.

FUNGU 5

وَلَقَدْ اٰتَيْنَا مُوْسَى الْكِتٰبَ مِنْۢ بَعْدِ مَآ اَهْلَكْنَا الْقُرُوْنَ الْاُوْلٰى بَصَآئِرَ لِلنَّاسِ وَهُدًى وَّرَحْمَةً لَّعَلَّهُمْ يَتَذَكَّرُوْنَ ﴿۴۴﴾

44. Na bila shaka Tulimpa Musa Kitabu baada ya kuviangamiza vizazi vya kwanza, kiwaangazie watu na kiwe mwongozo na rehema, ili wapate kushika nasaha.

Aya 39. *Unijengee mnara.* Maneno haya Firauni aliyasema kwa kebehi.

وَمَا كُنْتَ بِجَانِبِ الْغَرْبِيِّ اِذْ قَضَيْنَآ اِلٰى
مُوْسَى الْاَمْرَ وَمَا كُنْتَ مِنَ الشّٰهِدِيْنَ ﴿٤٥﴾

45. Na hukuwa upande wa magharibi Tulipompelekea Musa amri wala hukuwa miongoni mwa walioshuhudia.

وَلٰكِنَّآ اَنْشَاْنَا قُرُوْنًا فَتَطَاوَلَ عَلَيْهِمُ
الْعُمُرُ ۚ وَمَا كُنْتَ ثَاوِيًا فِيْٓ اَهْلِ مَدْيَنَ
تَتْلُوْا عَلَيْهِمْ اٰيٰتِنَا ۙ وَلٰكِنَّا كُنَّا
مُرْسِلِيْنَ ﴿٤٦﴾

46. Walakini Sisi Tuliviumba vizazi na umri ukawa mrefu juu yao, wala hukuwa mkazi pamoja na watu wa Madiani, kuwasomea Aya Zetu, walakini Sisi Tulikuwa Tuwapelekeao (Mitume).

وَمَا كُنْتَ بِجَانِبِ الطُّوْرِ اِذْ نَادَيْنَا وَلٰكِنْ
رَّحْمَةً مِّنْ رَّبِّكَ لِتُنْذِرَ قَوْمًا مَّآ اَتٰىهُمْ مِّنْ
نَّذِيْرٍ مِّنْ قَبْلِكَ لَعَلَّهُمْ يَتَذَكَّرُوْنَ ﴿٤٧﴾

47. Wala hukuwa upande wa mlima Tuliponadi, lakini (kutumwa kwako) ni rehema ya Mola wako, ili uwaonye watu wasiofikiwa na mwonyaji kabla yako, huenda watashika nasaha.

وَلَوْلَآ اَنْ تُصِيْبَهُمْ مُّصِيْبَةٌ ۢ بِمَا قَدَّمَتْ
اَيْدِيْهِمْ فَيَقُوْلُوْا رَبَّنَا لَوْلَآ اَرْسَلْتَ اِلَيْنَا
رَسُوْلًا فَنَتَّبِعَ اٰيٰتِكَ وَنَكُوْنَ مِنَ
الْمُؤْمِنِيْنَ ﴿٤٨﴾

48. Na isije ukawafikia msiba kwa yale iliyoyatanguliza mikono yao, kisha waseme: Mola wetu! mbona hukutupelekea Mtume nasi tungefuata aya Zako na tungekuwa miongoni mwa walioamini?

فَلَمَّا جَآءَهُمُ الْحَقُّ مِنْ عِنْدِنَا قَالُوْا
لَوْلَآ اُوْتِيَ مِثْلَ مَآ اُوْتِيَ مُوْسٰى ۭ اَوَلَمْ
يَكْفُرُوْا بِمَآ اُوْتِيَ مُوْسٰى مِنْ قَبْلُ ۚ قَالُوْا
سِحْرٰنِ تَظٰهَرَا ۡ وَقَالُوْٓا اِنَّا بِكُلٍّ
كٰفِرُوْنَ ﴿٤٩﴾

49. Lakini ilipowafikia haki kutoka Kwetu, wakasema: Mbona hukupewa kama yale aliyopewa Musa? Je, hawakuyakataa yale aliyopewa Musa zamani? Walisema: Ni wachawi wawili wanaosaidiana; na wakasema: Hakika sisi wote tunawakataa.

Aya 48. Jibu la swali hili ni lenye kuashiriwa, na sababu inayowafanya wao wasiweze kumlaumu Allah ni hii ya kwamba mara kwa mara Allah Huleta waonyaji kwa watu kabla ya kuwaadhibu kwa ajili ya vitendo vyao vibaya. Tazama sura ya 6 aya ya 132.

Aya 49. Miongoni mwa wapinzani wakuu watatu wa Islam - Wayahudi, Wakristo na waabudu sanamu - Wayahudi ndio wanaozungumziwa katika aya hii. Kauli hii ingeweza kutolewa na Wayahudi tu. Qur'an Tukufu inaposema kwamba waliyakataa yale aliyopewa Musa hapo zamani, haingekuwa na maana kwamba watu wa zama za Mtukufu Mtume wa Islam walimkataa Musa.

Ile sehemu ya aya yenye maneno *inna bikulliin kaafiruun* (tunawakataa wote) ina maana pia kwamba 'tunawakataa wale wote wanaokuja kwa jina la Allah na kile kinachoitwa Ishara'. Hii inaonyesha kwa mkazo zaidi maradhi waliyonayo wote wale wanaomkataa Mtume wa zama zao.

قُلْ فَاْتُوْا بِكِتٰبٍ مِّنْ عِنْدِ اللّٰهِ هُوَ اَهْدٰى مِنْهُمَاۤ اَتَّبِعْهُ اِنْ كُنْتُمْ صٰدِقِيْنَ ﴿٥٠﴾

50. Sema: Basi leteni Kitabu kitokacho kwa Allah ambacho kina mwongozo ulio bora kuliko hivi viwili (Taurati na Qur'an) ili nikifuate kama ninyi ni wakweli.

فَاِنْ لَّمْ يَسْتَجِيْبُوْا لَكَ فَاعْلَمْ اَنَّمَا يَتَّبِعُوْنَ اَهْوَآءَهُمْ ؕ وَ مَنْ اَضَلُّ مِمَّنِ اتَّبَعَ هَوٰىهُ بِغَيْرِ هُدًى مِّنَ اللّٰهِ ؕ اِنَّ اللّٰهَ لَا يَهْدِى الْقَوْمَ الظّٰلِمِيْنَ ﴿٥١﴾ ع ۸

51. Lakini kama hawakukujibu, basi jua ya kuwa wanajifuatia tu matamanio yao; na ni nani mpotevu zaidi kuliko yule anayejifuatia matamanio yake pasipo mwongozo utokao kwa Allah? Bila shaka Allah Hawaongozi watu wadhalimu.

FUNGU 6

وَلَقَدْ وَصَّلْنَا لَهُمُ الْقَوْلَ لَعَلَّهُمْ يَتَذَكَّرُوْنَ ﴿٥٢﴾ ؕ

52. Na kwa yakini Tuliwafululizia kauli ili wapate kushika nasaha.

اَلَّذِيْنَ اٰتَيْنٰهُمُ الْكِتٰبَ مِنْ قَبْلِهٖ هُمْ بِهٖ يُؤْمِنُوْنَ ﴿٥٣﴾

53. Wale Tuliowapa Kitabu kabla ya (Qur'an) hii wao wanaiamini.

وَ اِذَا يُتْلٰى عَلَيْهِمْ قَالُوْۤا اٰمَنَّا بِهٖۤ اِنَّهُ الْحَقُّ مِنْ رَّبِّنَاۤ اِنَّا كُنَّا مِنْ قَبْلِهٖ مُسْلِمِيْنَ ﴿٥٤﴾

54. Na wanaposomewa, husema: Tunaiamini, bila shaka hii ni haki itokayo kwa Mola wetu; kwa yakini kabla ya haya tulikuwa wajisalimishao.

اُولٰٓئِكَ يُؤْتَوْنَ اَجْرَهُمْ مَّرَّتَيْنِ بِمَا صَبَرُوْا وَ يَدْرَءُوْنَ بِالْحَسَنَةِ السَّيِّئَةَ وَ مِمَّا رَزَقْنٰهُمْ يُنْفِقُوْنَ ﴿٥٥﴾

55. Hao ndio watakaopewa ujira wao mara mbili kwa kuwa walisubiri; nao huondoa ubaya kwa wema, na hutoa katika yale Tuliyowapa.

وَ اِذَا سَمِعُوا اللَّغْوَ اَعْرَضُوْا عَنْهُ وَ قَالُوْا لَنَاۤ اَعْمَالُنَا وَ لَكُمْ اَعْمَالُكُمْ ۫ سَلٰمٌ عَلَيْكُمْ ۫ لَا نَبْتَغِى الْجٰهِلِيْنَ ﴿٥٦﴾

56. Na wanaposikia upuuzi hujitenga nao na husema: vitendo vyetu vitakuwa kwa ajili yetu na vitendo vyenu vitakuwa kwa ajili yenu, amani juu yenu, sisi hatuwataki wajinga.

اِنَّكَ لَا تَهْدِىْ مَنْ اَحْبَبْتَ وَ لٰكِنَّ اللّٰهَ يَهْدِىْ مَنْ يَّشَآءُ ۚ وَ هُوَ اَعْلَمُ

57. Kwa hakika wewe huwezi kumwongoza umpendaye, walakini

Aya 57. Inasimuliwa ya kwamba baba mdogo wa Mtume *s.a.w.* bwana Abu Talib, alipokuwa mgonjwa karibu kufa, Mtume *s.a.w.* alimbashiria na kumtaka aamini Allah. Lakini Abu Jahal alikuwa pale na akamkataza na kumwambia asiache dini ya baba zake. Basi

بِالْمُهْتَدِيْنَ ﴿٥٧﴾

Allah Humwongoza Amtakaye, naye ndiye Awajuaye sana waongokao.

وَقَالُوْٓا اِنْ نَّتَّبِعِ الْهُدٰى مَعَكَ نُتَخَطَّفْ مِنْ اَرْضِنَا ؕ اَوَلَمْ نُمَكِّنْ لَّهُمْ حَرَمًا اٰمِنًا يُّجْبٰٓى اِلَيْهِ ثَمَرٰتُ كُلِّ شَىْءٍ رِّزْقًا مِّنْ لَّدُنَّا وَلٰكِنَّ اَكْثَرَهُمْ لَا يَعْلَمُوْنَ ﴿٥٨﴾

58. Na wakasema: Kama tukifuata mwongozo pamoja nawe tutanyakuliwa kutoka nchi yetu. Je, Hatukuwakalisha mahali patakatifu na pa amani, yana kovutiwa matunda ya kila aina kuwa riziki itokayo Kwetu? Lakini wengi wao hawajui.

وَكَمْ اَهْلَكْنَا مِنْ قَرْيَةٍۭ بَطِرَتْ مَعِيْشَتَهَا ۚ فَتِلْكَ مَسٰكِنُهُمْ لَمْ تُسْكَنْ مِّنْۢ بَعْدِهِمْ اِلَّا قَلِيْلًا ؕ وَكُنَّا نَحْنُ الْوٰرِثِيْنَ ﴿٥٩﴾

59. Na Tumeingamiza miji mingapi iliyojifaharisha juu ya maisha yao! Hayo ni maskani yao yasiyokaliwa baada yao ila kidogo, na Sisi Tulikuwa Warithi.

وَمَا كَانَ رَبُّكَ مُهْلِكَ الْقُرٰى حَتّٰى يَبْعَثَ فِىْٓ اُمِّهَا رَسُوْلًا يَّتْلُوْا عَلَيْهِمْ اٰيٰتِنَا ۚ وَمَا كُنَّا مُهْلِكِى الْقُرٰٓى اِلَّا وَاَهْلُهَا ظٰلِمُوْنَ ﴿٦٠﴾

60. Na Mola wako Haangamizi mji mpaka Ampeleke Mtume katika mji wao mkuu, awasomee Aya Zetu; wala Hatuiangamizi miji mpaka watu wake wamekuwa wadhalimu.

وَمَآ اُوْتِيْتُمْ مِّنْ شَىْءٍ فَمَتَاعُ الْحَيٰوةِ الدُّنْيَا وَزِيْنَتُهَا ۚ وَمَا عِنْدَ اللّٰهِ خَيْرٌ وَّاَبْقٰى ؕ اَفَلَا تَعْقِلُوْنَ ﴿٦١﴾ ع ٩

61. Na cho chote mlichopewa, basi ni matumizi kwa maisha ya dunia na mapambo yake tu; lakini kilichoko kwa Allah ni bora na kitabaki; basi je, hamtumii akili?

FUNGU 7

اَفَمَنْ وَّعَدْنٰهُ وَعْدًا حَسَنًا فَهُوَ لَاقِيْهِ كَمَنْ مَّتَّعْنٰهُ مَتَاعَ الْحَيٰوةِ الدُّنْيَا ثُمَّ هُوَ

62. Je, mtu yule Tuliyemwahidi ahadi nzuri tena atakayoipata, anaweza kuwa sawa na yule Tuliyemnufaisha kwa

---

Bwana Abu Talib alikufa bila kuamini. Mtume s.a.w. alisikitika sana juu ya kutoamini kwake, na Allah aliteremsha Aya hii; hapo Mtume s.a.w. akapata kutulia.

Aya 61. Watu wanaoangukia anasa za dunia ingekuwa vema kwao kama wangekumbuka ya kuwa vitu vilivyoko kwa Allah ni bora zaidi kuliko hivi na watakaovipewa ni wale tu wanaoamini na kutenda wema.

Aya 62. Mambo yote ya dunia yanaendelea juu ya ahadi na nia safi. Tabia ya mwanadamu hufurahi anapopata ahadi kwa mtu mkubwa, mwaminifu. Hata inakuwa juu ya ahadi mambo

يَوْمَ الْقِيٰمَةِ مِنَ الْمُحْضَرِيْنَ ﴿٦٢﴾

manufaa ya maisha ya dunia, kisha siku ya Kiyama awe miongoni mwa waliohudhurishwa?

وَيَوْمَ يُنَادِيْهِمْ فَيَقُوْلُ اَيْنَ شُرَكَآءِيَ الَّذِيْنَ كُنْتُمْ تَزْعُمُوْنَ ﴿٦٣﴾

63. Na siku Atakapowaita. Atasema: Wako wapi washirika Wangu ambao mlikuwa mkiwadai?

قَالَ الَّذِيْنَ حَقَّ عَلَيْهِمُ الْقَوْلُ رَبَّنَا هٰٓؤُلَآءِ الَّذِيْنَ اَغْوَيْنَا ۚ اَغْوَيْنٰهُمْ كَمَا غَوَيْنَا ۚ تَبَرَّاْنَآ اِلَيْكَ ۖ مَا كَانُوْٓا اِيَّانَا يَعْبُدُوْنَ ﴿٦٤﴾

64. Watasema: wale iliyothibitika juu yao kauli: Mola wetu! hawa ndio Tuliowapoteza; tuliwapoteza kama tulivyopotea; tunajiepusha nao mbele Yako: hawakuwa wakituabudu sisi.

وَقِيْلَ ادْعُوْا شُرَكَآءَكُمْ فَدَعَوْهُمْ فَلَمْ يَسْتَجِيْبُوْا لَهُمْ وَرَاَوُا الْعَذَابَ ۚ لَوْ اَنَّهُمْ كَانُوْا يَهْتَدُوْنَ ﴿٦٥﴾

65. Na itasemwa: Waiteni washirika wenu. Basi watawaita lakini hawatawajibu, na wataiona adhabu; laiti wangalikuwa wenye kuongoka!

وَيَوْمَ يُنَادِيْهِمْ فَيَقُوْلُ مَاذَآ اَجَبْتُمُ الْمُرْسَلِيْنَ ﴿٦٦﴾

66. Na siku atakayowaita na Atasema: Je, mliwajibu nini Mitume?

فَعَمِيَتْ عَلَيْهِمُ الْاَنْۢبَآءُ يَوْمَئِذٍ فَهُمْ لَا يَتَسَآءَلُوْنَ ﴿٦٧﴾

67. Basi zitawapotea siku hiyo habari, nao hawataulizana.

فَاَمَّا مَنْ تَابَ وَاٰمَنَ وَعَمِلَ صَالِحًا فَعَسٰٓى اَنْ يَّكُوْنَ مِنَ الْمُفْلِحِيْنَ ﴿٦٨﴾

68. Basi ama aliyetubia na akaamini na akafanya vitendo vizuri, huenda akawa miongoni mwa wenye kufaulu.

وَرَبُّكَ يَخْلُقُ مَا يَشَآءُ وَيَخْتَارُ ۗ مَا كَانَ لَهُمُ الْخِيَرَةُ ۗ سُبْحٰنَ اللّٰهِ وَتَعٰلٰى عَمَّا يُشْرِكُوْنَ ﴿٦٩﴾

69. Na Mola wako Huumba Atakavyo na Huchagua: kwao hakuna hiari: Allah Ameepukana na upungufu, na Yu juu kabisa kuliko wale wawashirikishao naye.

وَرَبُّكَ يَعْلَمُ مَا تُكِنُّ صُدُوْرُهُمْ وَمَا يُعْلِنُوْنَ ﴿٧٠﴾

70. Na Mola wako Anayajua yanayoficha vifua vyao na wanayoyadhihirisha.

وَهُوَ اللّٰهُ لَآ اِلٰهَ اِلَّا هُوَ ۗ لَهُ الْحَمْدُ فِى الْاُوْلٰى وَالْاٰخِرَةِ ۖ وَلَهُ الْحُكْمُ وَاِلَيْهِ تُرْجَعُوْنَ ﴿٧٠﴾

71. Naye Ndiye Allah, hakuna aabudiwaye ila Yeye! Sifa zote njema - mwanzoni na mwishoni - ni Zake tu. Na hukumu pia ni Kwake, nanyi mtarudishwa Kwake.

mengi yanaendelea duniani. Je, siyo furaha ya ajabu kabisa inapokuwa ahadi njema imetolewa na Allah ambaye ni Mfalme wa wafalme.

72. Sema: Niambieni, kama Allah Akurefushieni usiku mpaka siku ya Kiyama, ni mungu gani asiyekuwa Allah atakayewaleteeni mwanga? Basi je, hamsikii?

قُلْ اَرَءَيْتُمْ اِنْ جَعَلَ اللّٰهُ عَلَيْكُمُ الَّيْلَ سَرْمَدًا اِلٰى يَوْمِ الْقِيٰمَةِ مَنْ اِلٰهٌ غَيْرُ اللّٰهِ يَاْتِيْكُمْ بِضِيَآءٍ ؕ اَفَلَا تَسْمَعُوْنَ ﴿٧٢﴾

73. Sema: Niambieni, kama Allah Akurefushieni mchana mpaka siku ya Kiyama, ni mungu gani asiyekuwa Allah atakayewaleteeni usiku, mnaopata humo utulivu ? Basi je, hamtumii busara?

قُلْ اَرَءَيْتُمْ اِنْ جَعَلَ اللّٰهُ عَلَيْكُمُ النَّهَارَ سَرْمَدًا اِلٰى يَوْمِ الْقِيٰمَةِ مَنْ اِلٰهٌ غَيْرُ اللّٰهِ يَاْتِيْكُمْ بِلَيْلٍ تَسْكُنُوْنَ فِيْهِ ؕ اَفَلَا تُبْصِرُوْنَ ﴿٧٣﴾

74. Na kwa rehema Zake Amewafanyieni usiku na mchana ili mtulie humo na mtafute fadhili Zake na ili mpate kushukuru.

وَمِنْ رَّحْمَتِهٖ جَعَلَ لَكُمُ الَّيْلَ وَالنَّهَارَ لِتَسْكُنُوْا فِيْهِ وَلِتَبْتَغُوْا مِنْ فَضْلِهٖ وَلَعَلَّكُمْ تَشْكُرُوْنَ ﴿٧٤﴾

75. Na siku Atakayowaita na kusema: Wako wapi washirika Wangu ambao mlikuwa mkidai?

وَيَوْمَ يُنَادِيْهِمْ فَيَقُوْلُ اَيْنَ شُرَكَآءِىَ الَّذِيْنَ كُنْتُمْ تَزْعُمُوْنَ ﴿٧٥﴾

76. Na Tutatoa katika kila umati shahidi na Tutasema: Leteni dalili zenu; ndipo watajua ya kwamba kweli iko kwa Allah na yatawapotea yale waliyokuwa wakiyazusha.

وَنَزَعْنَا مِنْ كُلِّ اُمَّةٍ شَهِيْدًا فَقُلْنَا هَاتُوْا بُرْهَانَكُمْ فَعَلِمُوْٓا اَنَّ الْحَقَّ لِلّٰهِ وَضَلَّ عَنْهُمْ مَّا كَانُوْا يَفْتَرُوْنَ ﴿٧٦﴾ ع ١٠

FUNGU 8

77. Hakika Karuni alikuwa katika watu wa Musa lakini aliwaasi. Na Tulimpa hazina ambazo funguo zake ziliwalemea kundi la watu wenye

اِنَّ قَارُوْنَ كَانَ مِنْ قَوْمِ مُوْسٰى فَبَغٰى عَلَيْهِمْ ۠ وَاٰتَيْنٰهُ مِنَ الْكُنُوْزِ مَآ اِنَّ مَفَاتِحَهٗ لَتَنُوْٓاُ بِالْعُصْبَةِ اُولِى الْقُوَّةِ ۗ

Aya 77. Mara nyingi mali humtia mtu kiburi na majivuno makubwa na kuwadharau watu; hata mali inamshawishi mtu kuendesha maovu ya namna nyingi na kuipinga haki na kuwaadui waaminio. Mali ya namna hii si mali ila ni balaa kwa ajili ya mwenye nayo. Kama vile Karuni, alipojivuna kwa mali zake asitake kuwasaidia wenye haki ya kusaidiwa basi Allah aliiangamiza mali yake. Lakini mali inapotumiwa kwa njia nzuri inakuwa baraka kubwa kwa mwenye nayo.

nguvu. Walipomwambia watu wake: Usijigambe, hakika Allah Hawapendi wanaojigamba.

78. Na utamani kuichuma nyumba ya Akhera kwa kupitia vile Alivyokupa Allah, wala usiisahau sehemu yako ya dunia, na ufanye wema kama Allah Alivyokufanyia wema, wala usitafute kufanya ufisadi katika nchi; bila shaka Allah Hawapendi wafisadi.

79. Akasema: Hakika nimepewa kwa sababu ya elimu niliyonayo. Je, hakujua ya kwamba Allah Amevangamiza kabla yake vizazi vingi waliokuwa wenye nguvu zaidi kuliko yeye na wenye mkusanyo mwingi zaidi? Na wakosefu hawataulizwa kwa makosa yao.

80. Basi akawatokea watu wake katika pambo lake. Wakasema wale wanaotaka maisha ya dunia: Laiti tungalipata kama alivyopewa Karuni; hakika yeye ni mwenye bahati kubwa.

81. Na wakasema wale waliopewa elimu: Ole wenu! Malipo ya Allah ni mazuri kwa yule anayeamini na kufanya vitendo vizuri, wala hawatayapewa isipokuwa wafanyao subira.

82. Basi Tukamdidimiza yeye na nyumba yake ardhini; na hakuwa na kundi la kumsaidia dhidi ya Allah, na wala hakuwa miongoni mwa wajilipizao kisasi.

83. Na wakaanza kusema wale waliotamani cheo chake jana: E-e-e (kweli) Allah Humzidishia riziki Amtakaye miongoni mwa

إِذْ قَالَ لَهٗ قَوْمُهٗ لَا تَفْرَحْ إِنَّ اللّٰهَ لَا يُحِبُّ الْفَرِحِيْنَ ﴿٧٧﴾

وَابْتَغِ فِيْمَآ اٰتٰىكَ اللّٰهُ الدَّارَ الْاٰخِرَةَ وَلَا تَنْسَ نَصِيْبَكَ مِنَ الدُّنْيَا وَاَحْسِنْ كَمَآ اَحْسَنَ اللّٰهُ اِلَيْكَ وَلَا تَبْغِ الْفَسَادَ فِي الْاَرْضِ ؕ اِنَّ اللّٰهَ لَا يُحِبُّ الْمُفْسِدِيْنَ ﴿٧٨﴾

قَالَ اِنَّمَآ اُوْتِيْتُهٗ عَلٰى عِلْمٍ عِنْدِيْ ؕ اَوَلَمْ يَعْلَمْ اَنَّ اللّٰهَ قَدْ اَهْلَكَ مِنْ قَبْلِهٖ مِنَ الْقُرُوْنِ مَنْ هُوَ اَشَدُّ مِنْهُ قُوَّةً وَّاَكْثَرُ جَمْعًا ؕ وَلَا يُسْـَٔلُ عَنْ ذُنُوْبِهِمُ الْمُجْرِمُوْنَ ﴿٧٩﴾

فَخَرَجَ عَلٰى قَوْمِهٖ فِيْ زِيْنَتِهٖ ؕ قَالَ الَّذِيْنَ يُرِيْدُوْنَ الْحَيٰوةَ الدُّنْيَا يٰلَيْتَ لَنَا مِثْلَ مَآ اُوْتِيَ قَارُوْنُ ۙ اِنَّهٗ لَذُوْ حَظٍّ عَظِيْمٍ ﴿٨٠﴾

وَقَالَ الَّذِيْنَ اُوْتُوا الْعِلْمَ وَيْلَكُمْ ثَوَابُ اللّٰهِ خَيْرٌ لِّمَنْ اٰمَنَ وَعَمِلَ صَالِحًا ۚ وَلَا يُلَقّٰىهَآ اِلَّا الصّٰبِرُوْنَ ﴿٨١﴾

فَخَسَفْنَا بِهٖ وَبِدَارِهِ الْاَرْضَ ۟ فَمَا كَانَ لَهٗ مِنْ فِئَةٍ يَّنْصُرُوْنَهٗ مِنْ دُوْنِ اللّٰهِ ۫ وَمَا كَانَ مِنَ الْمُنْتَصِرِيْنَ ﴿٨٢﴾

وَاَصْبَحَ الَّذِيْنَ تَمَنَّوْا مَكَانَهٗ بِالْاَمْسِ يَقُوْلُوْنَ وَيْكَاَنَّ اللّٰهَ يَبْسُطُ الرِّزْقَ لِمَنْ

يَّشَآءُ مِنۡ عِبَادِهٖ وَيَقۡدِرُ ۚ لَوۡلَاۤ اَنۡ مَّنَّ اللّٰهُ عَلَيۡنَا لَخَسَفَ بِنَا ؕ وَيۡكَاَنَّهٗ لَا يُفۡلِحُ الۡكٰفِرُوۡنَ ﴿۸۲﴾ ع ۱۱

watumishi Wake na Hudhikisha; Asingetufanyia hisani Allah bila shaka Angetudidimiza. Oh! wasioshukuru hawastawi.

FUNGU 9

تِلۡكَ الدَّارُ الۡاٰخِرَةُ نَجۡعَلُهَا لِلَّذِيۡنَ لَا يُرِيۡدُوۡنَ عُلُوًّا فِى الۡاَرۡضِ وَلَا فَسَادًا ؕ وَالۡعَاقِبَةُ لِلۡمُتَّقِيۡنَ ﴿۸۳﴾

84. Hiyo nyumba ya Akhera Tutawafanyia wale wasiotaka kujitukuza ardhini wala kufanya ufisadi, na mwisho (mwema) ni kwa wacha Mungu.

مَنۡ جَآءَ بِالۡحَسَنَةِ فَلَهٗ خَيۡرٌ مِّنۡهَا ۚ وَمَنۡ جَآءَ بِالسَّيِّئَةِ فَلَا يُجۡزَى الَّذِيۡنَ عَمِلُوا السَّيِّاٰتِ اِلَّا مَا كَانُوۡا يَعۡمَلُوۡنَ ﴿۸۴﴾

85. Atakayefanya wema atapata bora kuliko huo, na atakayefanya ubaya, basi hawatalipwa wale wafanyao ubaya ila yale waliyokuwa wakiyafanya·

اِنَّ الَّذِىۡ فَرَضَ عَلَيۡكَ الۡقُرۡاٰنَ لَرَآدُّكَ اِلٰى مَعَادٍ ؕ قُلۡ رَّبِّىۡۤ اَعۡلَمُ مَنۡ جَآءَ بِالۡهُدٰى وَمَنۡ هُوَ فِىۡ ضَلٰلٍ مُّبِيۡنٍ ﴿۸۵﴾

86. Hakika Yeye Aliyekufaradhishia Qur'an kwa yakini Atakurudisha mahali pa kurejea! Sema: Mola wangu ndiye Amjuaye sana ajaye na mwongozo na yule aliyomo katika upotevu dhahiri.

وَمَا كُنۡتَ تَرۡجُوۡۤا اَنۡ يُّلۡقٰۤى اِلَيۡكَ الۡكِتٰبُ اِلَّا رَحۡمَةً مِّنۡ رَّبِّكَ فَلَا تَكُوۡنَنَّ ظَهِيۡرًا لِّلۡكٰفِرِيۡنَ ﴿۸۶﴾

87. Nawe hukuwa unatumai ya kwamba utapelekewa Kitabu; lakini ni rehema ya Mola wako; basi usiwe msaidizi wa makafiri.

وَلَا يَصُدُّنَّكَ عَنۡ اٰيٰتِ اللّٰهِ بَعۡدَ اِذۡ اُنۡزِلَتۡ اِلَيۡكَ وَادۡعُ اِلٰى رَبِّكَ وَلَا تَكُوۡنَنَّ مِنَ الۡمُشۡرِكِيۡنَ ﴿۸۷﴾

88. Wala wasikuzuie (kuzifuata) Aya za Allah baada ya kufunuliwa kwako, na uwaite (watu) kwa Mola wako, wala usiwe miongoni mwa washirikina.

وَلَا تَدۡعُ مَعَ اللّٰهِ اِلٰهًا اٰخَرَ ۘ لَاۤ اِلٰهَ اِلَّا هُوَ ؕ كُلُّ شَىۡءٍ هَالِكٌ اِلَّا وَجۡهَهٗ ؕ لَهُ الۡحُكۡمُ وَاِلَيۡهِ تُرۡجَعُوۡنَ ﴿۸۸﴾ ع ۱۲

89. Wala usimwite pamoja na Allah, mungu mwingine; hakuna aabudiwaye ila Yeye; kila kitu kitaangamia isipokuwa Yeye; hukumu i Kwake na Kwake mtarejeshwa.

Aya 86. *Ma'aad,* Mahali pa kurejea," Aya hii ilishuka wakati Mtume *s.a.w.* anatoka Makka nayo ni bishara iliyotimia sawasawa, kwani Mtume baada ya kutoka Makka kwenda Madina baadaye alirudi Makka katika hali ya ushindi pamoja na watakatifu elfu kumi.

سُوْرَةُ الْعَنْكَبُوْتِ مَكِّيَّةٌ وَّ هِيَ مَعَ الْبَسْمَلَةِ سَبْعُوْنَ اٰيَةً وَّ سَبْعَةُ رُكُوْعَاتٍ

29. SURA AL-'ANKABUUT

Imeteremshwa Makka

Ina mafungu 7 na Aya 70 pamoja na Bismillahi

بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ ①

1. Kwa jina la Allah, Mwingi wa rehema, Mwingi wa ukarimu.

الٓمّٓ ②

2. Mimi ni Allah Nijuaye sana.

اَحَسِبَ النَّاسُ اَنْ يُّتْرَكُوْٓا اَنْ يَّقُوْلُوْٓا اٰمَنَّا وَهُمْ لَا يُفْتَنُوْنَ ③

3. Je, watu wanadhani wataachwa waseme tumeamini, nao hawatajaribiwa?

وَلَقَدْ فَتَنَّا الَّذِيْنَ مِنْ قَبْلِهِمْ فَلَيَعْلَمَنَّ اللّٰهُ الَّذِيْنَ صَدَقُوْا وَلَيَعْلَمَنَّ الْكٰذِبِيْنَ ④

4. Na bila shaka Tuliwajaribu wale waliokuwa kabla yao, na kwa yakini Allah Atawatambulisha wale wasemao kweli na Atawatambulisha wale wasemao uwongo.

اَمْ حَسِبَ الَّذِيْنَ يَعْمَلُوْنَ السَّيِّاٰتِ اَنْ يَّسْبِقُوْنَا ؕ سَآءَ مَا يَحْكُمُوْنَ ⑤

5. Je, wanadhania wale wafanyao maovu kwamba watatuepuka? Ni mabaya wanayoyahukumu.

مَنْ كَانَ يَرْجُوْا لِقَآءَ اللّٰهِ فَاِنَّ اَجَلَ اللّٰهِ لَاٰتٍ ؕ وَهُوَ السَّمِيْعُ الْعَلِيْمُ ⑥

6. Mwenye kutumaini kukutana na Allah, basi hakika muda uliopangwa na Allah ni wenye kufika; naye ni Mwenye kusikia, Mwenye kujua.

Sura hii imeitwa *Buibui* kwa sababu itikadi za uwongo na za ushirikina zimefananishwa na utando wa buibui katika sura hii Aya ya 42.

Aya 2. *Alif Laam* Miim (Tazama sura 2:2).

Aya 3. Allah hatosheki na imani ya mdomo tu. "Tumeamini." Bali hutaka atambulishe kwa kumjaribu mtu namna nyingi kuwa je ameamini kweli au ni maneno tu?

Inasimuliwa ya kwamba alikuwako Yahudi mmoja jina lake Abul Kheri. Alikuwa mtu mwaminifu anayemwamini Mungu mmoja. Siku moja alipita karibu na msikiti akamsikia mtoto anasoma Aya hii; *Aliif Laam Miim. Je watu wanadhani wataachwa waseme, Tumeamini, nao wasijaribiwe?* Mara Yahudi yule alianza kulia, akasogea na akaegemea ukuta wa msikiti na akalia sana. Usiku alipolala alimwona Mtume s.a.w. katika ndoto anamwambia; "Ee Abul Kheri: Mimi nastaajabu sana. Mtu mwenye elimu kama wewe hunikubali na kuingia katika dini ya Kiislamu?" Alipoamka Abul Kheri alitangaza ya kuwa yeye ameingia dini ya Kiislamu.

وَ مَنۡ جَاهَدَ فَاِنَّمَا يُجَاهِدُ لِنَفۡسِهٖ ؕ
اِنَّ اللّٰهَ لَغَنِىٌّ عَنِ الۡعٰلَمِيۡنَ ۝٧

7. Na anayejitahidi, basi bila shaka hujitahidi kwa ajili ya nafsi yake; kwa hakika Allah si mhitaji kwa walimwengu.

وَالَّذِيۡنَ اٰمَنُوۡا وَ عَمِلُوا الصّٰلِحٰتِ
لَنُكَفِّرَنَّ عَنۡهُمۡ سَيِّاٰتِهِمۡ وَ لَنَجۡزِيَنَّهُمۡ
اَحۡسَنَ الَّذِىۡ كَانُوۡا يَعۡمَلُوۡنَ ۝٨

8. Na walioamini na kufanya vitendo vizuri, kwa yakini Tutawaondolea maovu yao, na Tutawalipa mema ya yale waliyokuwa wakiyafanya.

وَوَصَّيۡنَا الۡاِنۡسَانَ بِوَالِدَيۡهِ حُسۡنًا ؕ وَاِنۡ
جَاهَدٰكَ لِتُشۡرِكَ بِىۡ مَا لَيۡسَ لَكَ بِهٖ
عِلۡمٌ فَلَا تُطِعۡهُمَا ؕ اِلَىَّ مَرۡجِعُكُمۡ
فَاُنَبِّئُكُمۡ بِمَا كُنۡتُمۡ تَعۡمَلُوۡنَ ۝٩

9. Na Tumemwusia mwanadamu (afanye) wema kwa wazazi wake; na kama wakikushurutisha kunishirikisha na yale usiyo na elimu nayo, basi usiwatii; Kwangu ni marudio yenu, basi Nitawaambieni mliyokuwa mkiyatenda.

وَالَّذِيۡنَ اٰمَنُوۡا وَعَمِلُوا الصّٰلِحٰتِ
لَنُدۡخِلَنَّهُمۡ فِى الصّٰلِحِيۡنَ ۝١٠

10. Na walioamini na wakafanya vitendo vizuri bila shaka Tutawaingiza katika watu wema.

وَ مِنَ النَّاسِ مَنۡ يَّقُوۡلُ اٰمَنَّا بِاللّٰهِ فَاِذَاۤ
اُوۡذِىَ فِى اللّٰهِ جَعَلَ فِتۡنَةَ النَّاسِ كَعَذَابِ
اللّٰهِ ؕ وَلَئِنۡ جَآءَ نَصۡرٌ مِّنۡ رَّبِّكَ لَيَقُوۡلُنَّ
اِنَّا كُنَّا مَعَكُمۡ ؕ اَوَلَيۡسَ اللّٰهُ بِاَعۡلَمَ بِمَا فِىۡ
صُدُوۡرِ الۡعٰلَمِيۡنَ ۝١١

11. Na katika watu wako wasemao: Tumemwamini Allah, lakini wanapoudhiwa katika (njia ya) Allah huifanya fitina ya watu kama ndio adhabu ya Allah; na kama ukifika msaada kutoka kwa Mola wako kwa yakini husema: Bila shaka sisi tulikuwa pamoja nanyi. Je, Allah hajui yaliyomo vifuani mwa walimwengu?

وَلَيَعۡلَمَنَّ اللّٰهُ الَّذِيۡنَ اٰمَنُوۡا وَلَيَعۡلَمَنَّ
الۡمُنٰفِقِيۡنَ ۝١٢

12. Na hakika Allah Atawatambulisha wale walioamini, na hakika Atawatambulisha wanafiki.

وَقَالَ الَّذِيۡنَ كَفَرُوۡا لِلَّذِيۡنَ اٰمَنُوا اتَّبِعُوۡا
سَبِيۡلَنَا وَلۡنَحۡمِلۡ خَطٰيٰكُمۡ ؕ وَمَا هُمۡ
بِحٰمِلِيۡنَ مِنۡ خَطٰيٰهُمۡ مِّنۡ شَىۡءٍ ؕ
اِنَّهُمۡ لَكٰذِبُوۡنَ ۝١٣

13. Na waliokufuru walisema kuwaambia walioamini: Fuateni njia yetu nasi tutayabeba makosa yenu; lakini hawataweza kubeba katika makosa yao cho chote; hakika wao ni waongo tu.

Aya 9. Allah anataka watu wawatii wazazi wao na wawaheshimu. Lakini kama wazazi watajiingiza katika mambo ya dini na kutaka kumkataza mtoto wao katika haki, basi hapo hakuna haki kuwatii, bali ni lazima kukataa maneno yao, maana Mwumba ana haki zaidi ya kutiiwa kuliko wao.

وَلَيَحْمِلُنَّ اَثْقَالَهُمْ وَاَثْقَالًا مَّعَ اَثْقَالِهِمْ ۫ وَلَيُسْـَٔلُنَّ يَوْمَ الْقِيٰمَةِ عَمَّا كَانُوْا يَفْتَرُوْنَ ﴿١٣﴾ ع

14. Bali kwa hakika watabeba mizigo yao na pia mizigo mingine isiyokuwa yao, na kwa yakini wataulizwa siku ya Kiyama juu ya yale waliyokuwa wakiyazua.

FUNGU 2

وَلَقَدْ اَرْسَلْنَا نُوْحًا اِلٰى قَوْمِهٖ فَلَبِثَ فِيْهِمْ اَلْفَ سَنَةٍ اِلَّا خَمْسِيْنَ عَامًا ؕ فَاَخَذَهُمُ الطُّوْفَانُ وَهُمْ ظٰلِمُوْنَ ﴿١٤﴾

15. Na bila shaka Tulimtuma Nuhu kwa watu wake na akakaa kati yao miaka elfu kasoro miaka hamsini; basi tufani likawashika hali wakiwa wadhalimu.

فَاَنْجَيْنٰهُ وَاَصْحٰبَ السَّفِيْنَةِ وَجَعَلْنٰهَاۤ اٰيَةً لِّلْعٰلَمِيْنَ ﴿١٥﴾

16. Na Tukamwokoa yeye na watu (waliokuwa naye) katika safina, na Tukaifanya (iwe) Ishara kwa walimwengu.

وَاِبْرٰهِيْمَ اِذْ قَالَ لِقَوْمِهِ اعْبُدُوا اللّٰهَ وَاتَّقُوْهُ ؕ ذٰلِكُمْ خَيْرٌ لَّكُمْ اِنْ كُنْتُمْ تَعْلَمُوْنَ ﴿١٦﴾

17. Na Ibrahimu alipowaambia watu wake: Mwabuduni Allah na Mcheni; hayo ni heri kwenu ikiwa mnajua.

اِنَّمَا تَعْبُدُوْنَ مِنْ دُوْنِ اللّٰهِ اَوْثَانًا وَّتَخْلُقُوْنَ اِفْكًا ؕ اِنَّ الَّذِيْنَ تَعْبُدُوْنَ مِنْ دُوْنِ اللّٰهِ لَا يَمْلِكُوْنَ لَكُمْ رِزْقًا فَابْتَغُوْا عِنْدَ اللّٰهِ الرِّزْقَ وَاعْبُدُوْهُ وَاشْكُرُوْا لَهٗ ؕ اِلَيْهِ تُرْجَعُوْنَ ﴿١٧﴾

18. Hakika ninyi mnayaabudu masanamu kinyume cha Allah, na mnatengeneza uwongo; bila shaka wale mnaowaabudu kinyume cha Allah wao hawaimiliki riziki yenu, kwa hiyo tafuteni riziki kwa Allah, na Mwabuduni na Mshukuruni, Kwake mtarejeshwa.

وَاِنْ تُكَذِّبُوْا فَقَدْ كَذَّبَ اُمَمٌ مِّنْ قَبْلِكُمْ ؕ وَمَا عَلَى الرَّسُوْلِ اِلَّا الْبَلٰغُ الْمُبِيْنُ ﴿١٨﴾

19. Na kama mkikadhibisha, basi wamekwisha kadhibisha watu wa kabla yenu. Na si juu ya Mtume ila kufikisha (ujumbe) waziwazi.

اَوَلَمْ يَرَوْا كَيْفَ يُبْدِئُ اللّٰهُ الْخَلْقَ ثُمَّ يُعِيْدُهٗ ؕ اِنَّ ذٰلِكَ عَلَى اللّٰهِ يَسِيْرٌ ﴿١٩﴾

20. Je, hawaoni jinsi Allah Aanzishavyo kiumbe kisha Anakirudisha mara ya pili? Hakika hayo kwa Allah ni rahisi.

Aya 14. *Na mizigo mingine.* Hii mizigo mingine kwa hakika ni mizigo yao wenyewe, maana wao wamewapoteza watu lazima wapate dhambi za kuwapoteza huko. Siyo maana yake kuwa watabebeshwa dhambi za watu wengine, kama wasemavyo Wakristo kuwa Yesu alichukua dhambi za wakosefu na akaadhibiwa badala yao.

قُلْ سِيْرُوْا فِي الْاَرْضِ فَانْظُرُوْا كَيْفَ بَدَاَ الْخَلْقَ ثُمَّ اللّٰهُ يُنْشِئُ النَّشْاَةَ الْاٰخِرَةَ ؕ اِنَّ اللّٰهَ عَلٰى كُلِّ شَيْءٍ قَدِيْرٌ ۚ﴿٢٠﴾

21. Sema: Tembeeni katika ardhi na tazameni jinsi Alivyoanzisha kuumba, kisha Allah Ndiye Atakayeumba umbo la baadaye. Bila shaka Allah ni Mwenye uwezo juu ya vitu vyote.

يُعَذِّبُ مَنْ يَّشَآءُ وَ يَرْحَمُ مَنْ يَّشَآءُ ۚ وَ اِلَيْهِ تُقْلَبُوْنَ ﴿٢١﴾

22. Humwadhibu Amtakaye na Humrehemu Amtakaye, na mtageuziwa Kwake.

وَ مَاۤ اَنْتُمْ بِمُعْجِزِيْنَ فِي الْاَرْضِ وَلَا فِي السَّمَآءِ ۫ وَ مَا لَكُمْ مِّنْ دُوْنِ اللّٰهِ مِنْ وَّلِيٍّ وَّ لَا نَصِيْرٍ ﴿٢٢﴾ ع

23. Na ninyi hamwezi kumdhoofisha ardhini wala mbinguni, nanyi hamna mlinzi wala msaidizi kinyume cha Allah.

FUNGU 3

وَالَّذِيْنَ كَفَرُوْا بِاٰيٰتِ اللّٰهِ وَ لِقَآئِهٖۤ اُولٰٓئِكَ يَئِسُوْا مِنْ رَّحْمَتِيْ وَ اُولٰٓئِكَ لَهُمْ عَذَابٌ اَلِيْمٌ ﴿٢٣﴾

24. Na wale waliozikataa Aya za Allah na mkutano Wake, hao ndio wenye kukata tamaa na rehema Yangu, na hao ndio watakaopata adhabu iumizayo.

فَمَا كَانَ جَوَابَ قَوْمِهٖۤ اِلَّاۤ اَنْ قَالُوا اقْتُلُوْهُ اَوْ حَرِّقُوْهُ فَاَنْجٰىهُ اللّٰهُ مِنَ النَّارِ ؕ اِنَّ فِيْ ذٰلِكَ لَاٰيٰتٍ لِّقَوْمٍ يُّؤْمِنُوْنَ ﴿٢٤﴾

25. Basi halikuwa jawabu la watu wake ila kusema: Mwueni au muunguzeni. Lakini Allah Akamwokoa katika moto. Bila shaka katika hayo zimo Ishara kwa watu weye kuamini.

وَقَالَ اِنَّمَا اتَّخَذْتُمْ مِّنْ دُوْنِ اللّٰهِ اَوْثَانًا ۙ مَّوَدَّةَ بَيْنِكُمْ فِي الْحَيٰوةِ الدُّنْيَا ۚ ثُمَّ يَوْمَ الْقِيٰمَةِ يَكْفُرُ بَعْضُكُمْ بِبَعْضٍ وَّ يَلْعَنُ

26. Na alisema: Hakika ninyi mmeshika masanamu badala ya Allah kwa kupendana baina yenu katika maisha ya dunia, lakini siku ya

Aya 21. Tukio hilo hilo limewasilishwa katika aya nyingine inayofanana na hii, aya ya 48 ya Suuratun Najm, kukiwako na badiliko dogo katika uchaguzi wa neno. Badala ya *aakhirah* neno linalotumika katika aya ile ni *ukhraa*. *Aakhir* laweza kutafsiriwa kwa maana ya baadaye na *ukhraa* lina maana ya nyingine. Kwa hiyo ni dhahiri kwamba maneno *ukhraa* na *aakhir* yanapochanganywa yatakuwa na maana ya aina nyingine ya umbo katika siku za baadaye.

Aya 26. Kwa kweli watu hudumu na mambo ya mila kama kuabudu masanamu na kutambikia mizimu kwa sababu ya kupendana na kutaka kuridhishana. Basi wanaonywa hapa ya kuwa mwenendo huu utawaletea taabu na adhabu mbele ya Allah. Wanachotakiwa ni kwamba wamtangulize Allah kuliko vitu vyote.

بَعْضُكُمْ بَعْضًا ۖ وَّمَاْوٰىكُمُ النَّارُ وَمَا لَكُمْ مِّنْ نّٰصِرِيْنَ ﴿٢٥﴾

Kiyama mtakataana wenyewe kwa wenyewe na mtalaaniana ninyi kwa ninyi, na makao yenu yatakuwa Motoni; na hamtapata wasaidizi wo wote.

فَاٰمَنَ لَهٗ لُوْطٌ ۘ وَقَالَ اِنِّيْ مُهَاجِرٌ اِلٰى رَبِّيْ ۭ اِنَّهٗ هُوَ الْعَزِيْزُ الْحَكِيْمُ ﴿٢٦﴾

27. Basi Luti akamwamini. Na (Ibrahimu) akasema: Hakika mimi nahamia kwa Mola wangu, bila shaka yeye ndiye Mwenye nguvu, Mwenye hekima.

وَوَهَبْنَا لَهٗٓ اِسْحٰقَ وَيَعْقُوْبَ وَجَعَلْنَا فِيْ ذُرِّيَّتِهِ النُّبُوَّةَ وَالْكِتٰبَ وَاٰتَيْنٰهُ اَجْرَهٗ فِي الدُّنْيَا ۚ وَاِنَّهٗ فِي الْاٰخِرَةِ لَمِنَ الصّٰلِحِيْنَ ﴿٢٧﴾

28. Na Tulimpa Isihaka na Yakubu, na Tukauweka katika kizazi chake Unabii na Kitabu, na Tukampa ujira wake katika dunia; naye katika Akhera kwa yakini atakuwa miongoni mwa watu wema.

وَلُوْطًا اِذْ قَالَ لِقَوْمِهٖٓ اِنَّكُمْ لَتَاْتُوْنَ الْفَاحِشَةَ ۡ مَا سَبَقَكُمْ بِهَا مِنْ اَحَدٍ مِّنَ الْعٰلَمِيْنَ ﴿٢٨﴾

29. Na Luti alipowaambia watu wake: Bila shaka ninyi mnafanya uovu (ambao) hakuna aliyewapiteni kwa (uovu) huo katika walimwengu.

اَىِٕنَّكُمْ لَتَاْتُوْنَ الرِّجَالَ وَتَقْطَعُوْنَ السَّبِيْلَ ۙ وَتَاْتُوْنَ فِيْ نَادِيْكُمُ الْمُنْكَرَ ۭ فَمَا كَانَ جَوَابَ قَوْمِهٖٓ اِلَّآ اَنْ قَالُوا ائْتِنَا بِعَذَابِ اللّٰهِ اِنْ كُنْتَ مِنَ الصّٰدِقِيْنَ ﴿٢٩﴾

30. Je, mnawaingilia wanaume, na kufanya ujambazi, na mnafanya maovu katika makusanyiko yenu? Basi hali-kuwa jawabu la watu wake ila kusema: Utuletee adhabu ya Allah ikiwa u miongoni mwa wasemao kweli!

قَالَ رَبِّ انْصُرْنِيْ عَلَى الْقَوْمِ الْمُفْسِدِيْنَ ﴿٣٠﴾ ع

31. Akasema: Mola wangu, Unisaidie juu ya watu wafisadi.

FUNGU 4

وَلَمَّا جَاۗءَتْ رُسُلُنَآ اِبْرٰهِيْمَ بِالْبُشْرٰى ۙ قَالُوْٓا اِنَّا مُهْلِكُوْٓا اَهْلِ هٰذِهِ الْقَرْيَةِ ۚ اِنَّ اَهْلَهَا كَانُوْا ظٰلِمِيْنَ ﴿٣١﴾

32. Na Wajumbe Wetu walipomjia Ibrahimu na habari njema, wakasema: Bila shaka tutawaangamiza wenyeji wa mji huu; hakika wenyeji wake wamekuwa wadhalimu.

قَالَ اِنَّ فِيْهَا لُوْطًا ۭ قَالُوْا نَحْنُ اَعْلَمُ بِمَنْ فِيْهَا ۡ لَنُنَجِّيَنَّهٗ وَاَهْلَهٗٓ اِلَّا امْرَاَتَهٗ ۡ كَانَتْ مِنَ الْغٰبِرِيْنَ ﴿٣٢﴾

33. Akasema: Hakika humo yumo Luti. Wakasema: Sisi tunajua sana aliyomo humo, kwa yakini tutamwokoa yeye na ahali zake ila mkewe aliye miongoni mwa wakaao nyuma.

34. Na wajumbe Wetu walipomfikia Luti, aliwahuzunikia, na moyo wake ulipata dhiki kwa ajili yao, nao wakasema: Usiogope wala usihuzunike, bila shaka sisi tutakuokoa wewe na ahali zako ila mke wako aliye miongoni mwa wakaao nyuma.

وَلَمَّآ اَنْ جَآءَتْ رُسُلُنَا لُوْطًا سِيْٓءَ بِهِمْ وَضَاقَ بِهِمْ ذَرْعًا وَّ قَالُوْا لَا تَخَفْ وَلَا تَحْزَنْ ۫ اِنَّا مُنَجُّوْكَ وَاَهْلَكَ اِلَّا امْرَاَتَكَ كَانَتْ مِنَ الْغٰبِرِيْنَ ﴿٣٤﴾

35. Kwa yakini sisi tutateremsha juu ya wenyeji wa mji huu adhabu kutoka mbinguni kwa sababu walikuwa wakiasi.

اِنَّا مُنْزِلُوْنَ عَلٰٓى اَهْلِ هٰذِهِ الْقَرْيَةِ رِجْزًا مِّنَ السَّمَآءِ بِمَا كَانُوْا يَفْسُقُوْنَ ﴿٣٥﴾

36. Na bila shaka Tumeacha katika huo Ishara wazi kwa watu wanaofahamu.

وَلَقَدْ تَّرَكْنَا مِنْهَآ اٰيَةًۢ بَيِّنَةً لِّقَوْمٍ يَّعْقِلُوْنَ ﴿٣٦﴾

37. Na kwa Madiani (Tulimtuma) ndugu yao Shuaibu, naye akasema: Enyi watu wangu, Mwabuduni Allah na itarajini siku ya Akhera wala msitembee katika ardhi mkifisidi.

وَاِلٰى مَدْيَنَ اَخَاهُمْ شُعَيْبًا ۙ فَقَالَ يٰقَوْمِ اعْبُدُوا اللّٰهَ وَارْجُوا الْيَوْمَ الْاٰخِرَ وَلَا تَعْثَوْا فِى الْاَرْضِ مُفْسِدِيْنَ ﴿٣٧﴾

38. Lakini wakamkadhibisha, basi likawashika tetemeko la nchi na wakawa ndani ya nyumba zao wenye kuanguka kifudifudi.

فَكَذَّبُوْهُ فَاَخَذَتْهُمُ الرَّجْفَةُ فَاَصْبَحُوْا فِىْ دَارِهِمْ جٰثِمِيْنَ ﴿٣٨﴾

39. Na pia Waadi na Wathamudi. Na hakika maskani zao zimewabainikieni; na Shetani aliwapambia vitendo vyao, na akawazuilia njia hali walikuwa wakiona vizuri.

وَعَادًا وَّثَمُوْدَا۟ وَقَدْ تَّبَيَّنَ لَكُمْ مِّنْ مَّسٰكِنِهِمْ ۫ وَزَيَّنَ لَهُمُ الشَّيْطٰنُ اَعْمَالَهُمْ فَصَدَّهُمْ عَنِ السَّبِيْلِ وَكَانُوْا مُسْتَبْصِرِيْنَ ﴿٣٩﴾

40. Na (vile vile) Karuni, na Firauni na Hamana; na hakika aliwafikia Musa na Ishara waziwazi, lakini walijivuna katika ardhi, wala hawakuwa wenye kupita (nje ya adhabu yetu).

وَقَارُوْنَ وَفِرْعَوْنَ وَهَامٰنَ ۫ وَلَقَدْ جَآءَهُمْ مُّوْسٰى بِالْبَيِّنٰتِ فَاسْتَكْبَرُوْا فِى الْاَرْضِ وَمَا كَانُوْا سٰبِقِيْنَ ﴿٤٠﴾

41. Basi kila mmoja Tulimkamata kwa sababu ya dhambi yake: miongoni mwao yuko Tuliyempelekea kimbunga cha changarawe; na miongoni mwao yuko iliyemshika ngurumo; na miongoni mwao yuko Tuliyemdidimiza ardhini; na

فَكُلًّا اَخَذْنَا بِذَنْۢبِهٖ ۚ فَمِنْهُمْ مَّنْ اَرْسَلْنَا عَلَيْهِ حَاصِبًا ۚ وَمِنْهُمْ مَّنْ اَخَذَتْهُ الصَّيْحَةُ ۚ وَمِنْهُمْ مَّنْ خَسَفْنَا بِهِ الْاَرْضَ ۚ وَمِنْهُمْ مَّنْ اَغْرَقْنَا ۚ

miongoni mwao yuko Tuliyemgharikisha. Na Hakuwa Allah wa kuwadhulumu, walakini walikuwa wakijidhulumu wenyewe.

وَمَا كَانَ اللّٰهُ لِيَظْلِمَهُمْ وَلٰكِنْ كَانُوْٓا اَنْفُسَهُمْ يَظْلِمُوْنَ ﴿٤١﴾

42. Mfano wa wale waliofanya marafiki kinyume cha Allah ni kama mfano wa buibui ajitandiaye nyumba; na bila shaka nyumba iliyo dhaifu kuliko zote ni nyumba ya buibui: laiti wangalijua!

مَثَلُ الَّذِيْنَ اتَّخَذُوْا مِنْ دُوْنِ اللّٰهِ اَوْلِيَآءَ كَمَثَلِ الْعَنْكَبُوْتِ ۚ اِتَّخَذَتْ بَيْتًا ؕ وَاِنَّ اَوْهَنَ الْبُيُوْتِ لَبَيْتُ الْعَنْكَبُوْتِ ۘ لَوْ كَانُوْا يَعْلَمُوْنَ ﴿٤٢﴾

43. Kwa yakini Allah Huyajua wanayoyaita badala Yake; naye ndiye Mwenye ushindi kamili, Mwenye hekima.

اِنَّ اللّٰهَ يَعْلَمُ مَا يَدْعُوْنَ مِنْ دُوْنِهٖ مِنْ شَىْءٍ ؕ وَهُوَ الْعَزِيْزُ الْحَكِيْمُ ﴿٤٣﴾

44. Na hiyo ndiyo mifano Tunayoieleza kwa watu, na hawaifahamu ila wajuao.

وَتِلْكَ الْاَمْثَالُ نَضْرِبُهَا لِلنَّاسِ ۚ وَمَا يَعْقِلُهَآ اِلَّا الْعٰلِمُوْنَ ﴿٤٤﴾

45. Allah Ameziumba mbingu na ardhi kwa haki. Kwa hakika katika hayo zimo Ishara kwa waaminio.

خَلَقَ اللّٰهُ السَّمٰوٰتِ وَالْاَرْضَ بِالْحَقِّ ؕ اِنَّ فِىْ ذٰلِكَ لَاٰيَةً لِّلْمُؤْمِنِيْنَ ﴿٤٥﴾ ع

JUZU 21

FUNGU 5

46. Soma uliyofunuliwa katika Kitabu na usimamishe Sala. Bila shaka Sala huzuia mambo ya aibu na maovu, na kwa yakini kumkumbuka Allah ni (jambo) kubwa kabisa. Na Allah Anayajua mnayoyatenda.

اُتْلُ مَآ اُوْحِىَ اِلَيْكَ مِنَ الْكِتٰبِ وَاَقِمِ الصَّلٰوةَ ؕ اِنَّ الصَّلٰوةَ تَنْهٰى عَنِ الْفَحْشَآءِ وَالْمُنْكَرِ ؕ وَلَذِكْرُ اللّٰهِ اَكْبَرُ ؕ وَاللّٰهُ يَعْلَمُ مَا تَصْنَعُوْنَ ﴿٤٦﴾

Aya 42. Kuwategemea mizimu na miungu wa uwongo, au kuwategemea marafiki wanokwenda kinyume na Allah ni sawa na kujikinga katika nyumba ya buibui maana haitafaa kitu.

Aya 46. *Sala huzuia mambo ya aibu na maovu.* Sifa mojawapo ya Qur'an ni hii ya kuwa haikatazi jambo lo lote wala haiamrishi jambo ila itatoa sababu. Hapa imeamrishwa Sala na sababu imetolewa kuwa Sala inamhifadhi mtu katika mambo ya aibu na uovu. Mahali pengine Allah amesema, mioyo hupata utulivu kwa Sala (sura 13:29) na kwa Sala mtu hupata elimu ya yakini inayoondosha shaka yote, na inaipa roho maendeleo kama vile kulivyo na njia ya maendeleo katika mambo mbali mbali ya ulimwengu huu.

47. Wala msijadiliane na watu wa Kitabu ila kwa yale yaliyo bora, isipokuwa wale waliodhulumu miongoni mwao. Na semeni: Tunaamini yaliyoteremshwa kwetu na yaliyoteremshwa kwenu, na Mungu wetu na Mungu wenu ni Mmoja; nasi ni wajitupao Kwake.

وَلَا تُجَادِلُوْٓا اَهْلَ الْكِتٰبِ اِلَّا بِالَّتِيْ هِيَ اَحْسَنُ ۖ اِلَّا الَّذِيْنَ ظَلَمُوْا مِنْهُمْ وَقُوْلُوْٓا اٰمَنَّا بِالَّذِيْٓ اُنْزِلَ اِلَيْنَا وَاُنْزِلَ اِلَيْكُمْ وَاِلٰهُنَا وَاِلٰهُكُمْ وَاحِدٌ وَّنَحْنُ لَهٗ مُسْلِمُوْنَ ﴿٤٦﴾

48. Na kadhalika Tumekuteremshia Kitabu, basi wale Tuliowapa Kitabu wanakiamini, na miongoni mwa hawa yuko anayekiamini; na hawazipingi Aya Zetu isipokuwa makafiri.

وَكَذٰلِكَ اَنْزَلْنَآ اِلَيْكَ الْكِتٰبَ ۭ فَالَّذِيْنَ اٰتَيْنٰهُمُ الْكِتٰبَ يُؤْمِنُوْنَ بِهٖ ۚ وَمِنْ هٰٓؤُلَاۗءِ مَنْ يُّؤْمِنُ بِهٖ ۭ وَمَا يَجْحَدُ بِاٰيٰتِنَآ اِلَّا الْكٰفِرُوْنَ ﴿٤٧﴾

49. Na hukuwa mwenye kusoma kitabu cho chote kabla ya hiki, wala hukukiandika kwa mkono wako wa kuume, ndipo wangefanya shaka wabatilishao.

وَمَا كُنْتَ تَتْلُوْا مِنْ قَبْلِهٖ مِنْ كِتٰبٍ وَّلَا تَخُطُّهٗ بِيَمِيْنِكَ اِذًا لَّارْتَابَ الْمُبْطِلُوْنَ ﴿٤٨﴾

50. Bali hizi ni Aya waziwazi (zinazohifadhiwa) katika vifua vya wale waliopewa elimu; na hawazipingi Ishara Zetu isipokuwa wadhalimu.

بَلْ هُوَ اٰيٰتٌۢ بَيِّنٰتٌ فِيْ صُدُوْرِ الَّذِيْنَ اُوْتُوا الْعِلْمَ ۭ وَمَا يَجْحَدُ بِاٰيٰتِنَآ اِلَّا الظّٰلِمُوْنَ ﴿٤٩﴾

Imesimuliwa ya kwamba kijana mmoja katika Ansar wa Madina alikuwa akisali pamoja na Mtume *s.a.w.* lakini hakuwa na uovu aliokuwa haufanyi. Mtume *s.a.w.* alipopewa habari hii akasema, Hakika Sala yake itamwachisha maovu hayo. Naye hakukaa sana ila alitubu na akaacha maovu. (Baidhawi).

Kumbuko la Allah ni jambo kubwa kabisa. Maneno haya yanafasirika namna mbili: (1) Sala ndio hasa *dhikri* (kumbuko) kubwa; na (2) faida kubwa ya kusali ni kuwa kunamfanya mtu akumbukwe na Allah kwa kurehemewa.

Aya 47. *Isipokuwa wale waliodhulumu.* Watu wanaotaka kuleta ubishi wa ovyo na hawataki kuzungumza kwa njia nzuri hao tusijadiliane nao.

Aya 49. Aya hii inaonyesha ya kuwa Mtume *s.a.w.* alikuwa *ummi* yaani asiyejua kusoma wala kuandika. Hii bila shaka ni Ishara kubwa iliyo kinyume cha desturi ya kuwa mtu asiyepata kusoma atoe Kitabu kilichokusanya kila namna ya elimu zilizo tukufu.

Aya 50. Hapa Qur'an inanadi ya kuwa Aya zake zitahifadhiwa katika vifua vya wenye elimu na hata moja haitapotea. Toka siku ya mwanzo Qur'an ilihifadhika namna hii hata kulikuwa na watu walioijua yote kwa moyo na mpaka sasa wanapatikana kwa maelfu. Taurati na Injili ni Vitabu walivyokuwa navyo Mayahudi na Wakristo lakini havikuhifadhiwa namna hii (Shahaadatul Kuran).

وَقَالُوْا لَوْلَآ اُنْزِلَ عَلَيْهِ اٰيٰتٌ مِّنْ رَّبِّهٖ ؕ قُلْ اِنَّمَا الْاٰيٰتُ عِنْدَ اللّٰهِ ؕ وَاِنَّمَآ اَنَا نَذِيْرٌ مُّبِيْنٌ ۝۵۱

51. Na wakasema: Mbona hakuteremshiwa Ishara kutoka kwa Mola wake? Sema: Ishara zi Kwake Allah tu, nami hakika ni mwonyaji dhahiri.

اَوَلَمْ يَكْفِهِمْ اَنَّآ اَنْزَلْنَا عَلَيْكَ الْكِتٰبَ يُتْلٰى عَلَيْهِمْ ؕ اِنَّ فِيْ ذٰلِكَ لَرَحْمَةً وَّ ذِكْرٰى لِقَوْمٍ يُّؤْمِنُوْنَ ۝۵۲ ع

52. Je, hayakuwatosha ya kwamba Tumekuteremshia Kitabu wanachosomewa? Bila shaka katika hicho mna rehema na mauidha kwa watu wanaoamini.

FUNGU 6

قُلْ كَفٰى بِاللّٰهِ بَيْنِيْ وَبَيْنَكُمْ شَهِيْدًا ۚ يَعْلَمُ مَا فِي السَّمٰوٰتِ وَالْاَرْضِ ؕ وَالَّذِيْنَ اٰمَنُوْا بِالْبَاطِلِ وَكَفَرُوْا بِاللّٰهِ ۙ اُولٰٓئِكَ هُمُ الْخٰسِرُوْنَ ۝۵۳

53. Sema: Allah Anatosha kuwa Shahidi kati yangu na kati yenu. Anayajua yaliyomo katika mbingu na ardhi. Na wale wanaokubali batili na kumkataa Allah, hao ndio wapatao hasara.

وَيَسْتَعْجِلُوْنَكَ بِالْعَذَابِ ؕ وَلَوْلَآ اَجَلٌ مُّسَمًّى لَّجَآءَهُمُ الْعَذَابُ ؕ وَلَيَاْتِيَنَّهُمْ بَغْتَةً وَّهُمْ لَا يَشْعُرُوْنَ ۝۵۴

54. Na wanakuomba uilete adhabu haraka. Na kama pasingaliwekwa wakati maalumu, adhabu ingaliwafikia. Na kwa yakini itawafikia kwa ghafla nao hawatatambua.

يَسْتَعْجِلُوْنَكَ بِالْعَذَابِ ؕ وَ اِنَّ جَهَنَّمَ لَمُحِيْطَةٌ ۙ بِالْكٰفِرِيْنَ ۝۵۵ ۙ

55. Wanakuomba uilete adhabu haraka. Na hakika Jahannamu inawazunguka makafiri.

يَوْمَ يَغْشٰىهُمُ الْعَذَابُ مِنْ فَوْقِهِمْ وَمِنْ تَحْتِ اَرْجُلِهِمْ وَيَقُوْلُ ذُوْقُوْا مَا كُنْتُمْ

56. Siku itakapowafunika adhabu itokayo juu yao na chini ya miguu yao,

Aya 51. Ishara wanazosema makafiri kuwa hazikuteremshwa ni Ishara za adhabu. Wanajibiwa ya kuwa Ishara za namna hiyo pia ziko, lakini kwanza wanaonywa kwa Ishara za rehema (Aya 52), na kama hazitawatosheni hizi kwa sababu ya jeuri yenu basi zile za adhabu pia zitafika.

Tunashangaa kuona mapadre kwa sababu ya kutojua kwao wanaanza kuzifahamu Aya za namna hii kuwa zinaonyesha Mtume *s.a.w.* amekataa kuonyesha miujiza yo yote! Hazionyeshi hivi, kwani miujiza ya rehema ni mingi iliyooneshwa, lakini makafiri walitaka Ishara za adhabu, na wanajibiwa kuwa hata hivyo pia hizo ziko na zina wakati wake (tazama Aya 54).

Yesu ndiye hasa angefaa kusemwa kuwa hakuonyesha Ishara. Imeandikwa, "Wakatokea Mafarisayo, wakaanza kuhojiana naye; wakitafuta kwake Ishara itokayo mbinguni; wakimjaribu. Akaugua rohoni mwake, akasema, Mbona kizazi hiki chatafuta ishara? Amin, nawaambieni, *Hakitapewa ishara kizazi hiki"* (Marko 8:11-12.

Aya 56. Adhabu za namna hii zinazowatinga watu kabisa ndizo huwafika makafiri kila

تَعْمَلُوْنَ ﴿٥٦﴾

na Atasema: Onjeni mliyokuwa mkitenda.

يٰعِبَادِيَ الَّذِيْنَ اٰمَنُوْٓا اِنَّ اَرْضِيْ وَاسِعَةٌ فَاِيَّايَ فَاعْبُدُوْنِ ﴿٥٧﴾

57. Enyi watumishi Wangu mlioamini, kwa yakini ardhi Yangu ina wasaa, basi Mimi tu mniabudu.

كُلُّ نَفْسٍ ذَآئِقَةُ الْمَوْتِ ۫ ثُمَّ اِلَيْنَا تُرْجَعُوْنَ ﴿٥٨﴾

58. Kila nafsi ni yenye kuonja mauti, kisha mtarudishwa Kwetu.

وَالَّذِيْنَ اٰمَنُوْا وَعَمِلُوا الصّٰلِحٰتِ لَنُبَوِّئَنَّهُمْ مِّنَ الْجَنَّةِ غُرَفًا تَجْرِيْ مِنْ تَحْتِهَا الْاَنْهٰرُ خٰلِدِيْنَ فِيْهَا ؕ نِعْمَ اَجْرُ الْعٰمِلِيْنَ ﴿٥٩﴾

59. Na ambao wameamini na kufanya vitendo vizuri, bila shaka Tutawakalisha katika maghorofa ya Peponi mpitamo mito chini yake, wakikaa humo. Ni mwema ulioje ujira wa watendao (mema):

الَّذِيْنَ صَبَرُوْا وَعَلٰى رَبِّهِمْ يَتَوَكَّلُوْنَ ﴿٦٠﴾

60. Ambao walisubiri na kwa Mola wao wanatawakali.

وَكَاَيِّنْ مِّنْ دَآبَّةٍ لَّا تَحْمِلُ رِزْقَهَا ۖ اَللّٰهُ يَرْزُقُهَا وَاِيَّاكُمْ ۚ وَهُوَ السَّمِيْعُ الْعَلِيْمُ ﴿٦١﴾

61. Na wanyama wote watembeao ardhini hawabebi riziki zao? Allah Huwaruzuku wao na ninyi pia; naye ndiye Asikiaye, Ajuaye.

وَلَئِنْ سَاَلْتَهُمْ مَّنْ خَلَقَ السَّمٰوٰتِ وَالْاَرْضَ وَسَخَّرَ الشَّمْسَ وَالْقَمَرَ لَيَقُوْلُنَّ اللّٰهُ ۚ فَاَنّٰى يُؤْفَكُوْنَ ﴿٦٢﴾

62. Na kama ukiwauliza, Ni nani aliyeumba mbingu na ardhi na akavitiisha jua na mwezi? Bila shaka watasema, Allah. Wapi basi wanakogeuziwa?

اَللّٰهُ يَبْسُطُ الرِّزْقَ لِمَنْ يَّشَآءُ مِنْ عِبَادِهٖ وَيَقْدِرُ لَهٗ ؕ اِنَّ اللّٰهَ بِكُلِّ شَيْءٍ عَلِيْمٌ ﴿٦٣﴾

63. Allah Humkunjulia riziki Amtakaye katika watumishi Wake na Humdhikisha. Kwa hakika Allah ni Mjuzi wa kila kitu.

وَلَئِنْ سَاَلْتَهُمْ مَّنْ نَّزَّلَ مِنَ السَّمَآءِ مَآءً فَاَحْيَا بِهِ الْاَرْضَ مِنْۢ بَعْدِ مَوْتِهَا لَيَقُوْلُنَّ

64. Na ukiwauliza: Ni nani ateremshaye maji mawinguni na kuihuisha ardhi baada ya kufa kwake? Bila shaka

watasema: Allah. Sema: Sifa zote njema ni za Allah. Lakini wengi wao hawafahamu.

اللّٰهُ ؕ قُلِ الْحَمْدُ لِلّٰهِ ؕ بَلْ اَكْثَرُهُمْ لَا يَعْقِلُوْنَ ﴿۶۳﴾ ع ۴

FUNGU 7

65. Na maisha haya ya dunia hii siyo ila ni upuuzi na mchezo; na hakika nyumba ya Akhera ndiyo maisha hasa: laiti wangalijua!

وَمَا هٰذِهِ الْحَيٰوةُ الدُّنْيَاۤ اِلَّا لَهْوٌ وَّلَعِبٌ ؕ وَ اِنَّ الدَّارَ الْاٰخِرَةَ لَهِىَ الْحَيَوَانُ ۘ لَوْ كَانُوْا يَعْلَمُوْنَ ﴿۶۴﴾

66. Na wanapopanda katika merikebu, wanamwomba Allah wakimhalisishia utii. Lakini Anapowafikisha salama barani mara wanamshirikisha;

فَاِذَا رَكِبُوْا فِى الْفُلْكِ دَعَوُا اللّٰهَ مُخْلِصِيْنَ لَهُ الدِّيْنَ ۚ فَلَمَّا نَجّٰىهُمْ اِلَى الْبَرِّ اِذَا هُمْ يُشْرِكُوْنَ ﴿۶۵﴾

67. Wapate kutoshukuru kwa yale Tuliyowapa, na ili wajinufaishe kidogo. Hivyo karibuni watajua (matokeo yake)!

لِيَكْفُرُوْا بِمَاۤ اٰتَيْنٰهُمْ ۙ وَ لِيَتَمَتَّعُوْا ۟ فَسَوْفَ يَعْلَمُوْنَ ﴿۶۶﴾

68. Je, hawaoni ya kwamba Tumeifanya nchi takatifu kuwa na amani, hali hunyang'anywa watu wa pembezoni mwake? Je, wataamini batili na kuzikataa neema za Allah?

اَوَلَمْ يَرَوْا اَنَّا جَعَلْنَا حَرَمًا اٰمِنًا وَّيُتَخَطَّفُ النَّاسُ مِنْ حَوْلِهِمْ ؕ اَفَبِالْبَاطِلِ يُؤْمِنُوْنَ وَبِنِعْمَةِ اللّٰهِ يَكْفُرُوْنَ ﴿۶۷﴾

69. Na nani mdhalimu mkubwa kuliko yule anayemzushia uwongo Allah, au anayekadhibisha haki inapomjia? Je, si katika Jahannamu kao la makafiri?

وَمَنْ اَظْلَمُ مِمَّنِ افْتَرٰى عَلَى اللّٰهِ كَذِبًا اَوْ كَذَّبَ بِالْحَقِّ لَمَّا جَآءَهٗ ؕ اَلَيْسَ فِىْ جَهَنَّمَ مَثْوًى لِّلْكٰفِرِيْنَ ﴿۶۸﴾

Kama mtu mwenye imani anaihama nchi kwa sababu ya kuilinda imani yake, basi bila shaka Allah atamlipa mema na atampa raha. Mfano wa Masahaba unahakikisha jambo hili.

Aya 68. Nchi takatifu (Haraam) ni Makka na maili kadha wa kadha za ardhi inayoizunguka. Kuhifadhiwa kwa ardhi ya Makka ni mwujiza mkubwa. Nchi hii imehifadhiwa hata haiwezi kuingia katika mikono ya wasioiheshimu. Ijapokuwa unyang'anyi umetanda kila upande kuizunguka na kuuana na kupigana kunavumishwa, lakini kwa karne na karne nchi hii haikuondolewa staha yake, na watu humo wamekaa salama kabisa, ingawa makabila ya Waarabu walioizunguka yamo bado katika ujinga. Jambo hili hapana shaka linadhihirisha uwezo mkubwa wa Allah na ujuzi wake.

70. Na wale wanaojitahidi kwa ajili Yetu, kwa yakini Tunawaongoza kwenye njia Zetu. Na bila shaka Allah Yu pamoja na wafanyao mema.

وَالَّذِيْنَ جَاهَدُوْا فِيْنَا لَنَهْدِيَنَّهُمْ سُبُلَنَا ؕ
وَ اِنَّ اللّٰهَ لَمَعَ الْمُحْسِنِيْنَ ۝٦٩ ع

Aya 70. Juhudi hasa ni mahangaiko ya kweli, tamaa iliyo sahihi, juhudi kubwa, na kuomba dua. Huba tu bila juhudi haifai. Mtu anapotumia uwezo wake wote katika njia ya Allah basi Mungu humfanyia hisani akamwonyesha kila njia, na yale asiyoyaweza akamfanyia. Lakini siyo matlabu yake ya kuwa maji yanapatikana futi 12 chini, kisha mtu achimbe futi mbili tu na akae aseme amechoka. Bali juhudi kubwa ndiyo jambo la lazima kwa kumtafuta Allah.

سُوْرَةُ الرُّوْمِ مَكِّيَّةٌ وَّ هِيَ مَعَ الْبَسْمَلَةِ اِحْدٰى وَ سِتُّوْنَ اٰيَةً وَّ سِتَّةُ رُكُوْعَاتٍ

30. SURA AR-RUUM

Imeteremshwa Makka

Ina mafungu 6 na Aya 61 pamoja na Bismillahi

بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ ①

1. Kwa jina la Allah, Mwingi wa rehema, Mwingi wa ukarimu.

الٓمّٓ ②

2. Mimi ni Allah Nijuaye sana.

غُلِبَتِ الرُّوْمُ ③

3. Warumi wameshindwa.

فِيْٓ اَدْنَى الْاَرْضِ وَهُمْ مِّنْۢ بَعْدِ غَلَبِهِمْ سَيَغْلِبُوْنَ ④

4. Katika nchi iliyo karibu; nao baada ya kushindwa kwao, watashinda.

فِيْ بِضْعِ سِنِيْنَ ؕ لِلّٰهِ الْاَمْرُ مِنْ قَبْلُ وَمِنْۢ بَعْدُ ؕ وَيَوْمَئِذٍ يَّفْرَحُ الْمُؤْمِنُوْنَ ⑤

5. Katika miaka michache; Amri ni ya Allah kabla na baadaye; na siku hiyo waaminio watafurahi,

Sura hii imepata jina katika bishara ya maana inayoeleza kuwa Warumi watawashinda Waajemi ambao wakati ilipotolewa bishara hii wao Warumi walikuwa wameshindwa kabisa na milki zao zimekwisha ingia mikononi mwa Waajemi. Sura hii inajulikana kuwa ya Makka (Muhit) na ilishuka katika mwaka wa sita au wa saba kabla ya Hijra.

Aya 2. *Alif Laam Miim* (Tazama sura 2:2). Warumi ni watu wa zamani waliotawala milki kubwa. Mji wao mkubwa uliitwa Rumi (Rome) nao ulikuwa katika nchi ya Italia kando ya mto Tiber. Warumi waliona ni kudharauliwa kuitwa Magiriki (Wayunani) kwa vile jina hilo lilikuwa sawa na kumwita mtu mshenzi (Butler's Arab Conquest of Egypt, maelezo uk. 141). Hivyo kutafsiri Rumi kuwa Wayunani kama alivyofasiri Padre Dale si sawa, maana wenyewe walijiita Warumi.

Aya 4. *Nchi iliyo karibu* ni Shaam.

Aya 5. *Bidh'i siniin,* "miaka michache" Maneno haya huonyesha kitambo cha miaka 3 mpaka 9 (Baidhawi).

Kulikuwa ugomvi baina ya falme mbili - Rumi na Ajemi - ulioanza katika mwaka 602 A.D. Na katika mapigano hayo, Waajemi waliwashinda Warumi. Habari za kushinda Waajemi zilipofika Makka, makafiri wakafurahi sana, maana Waajemi walikuwa wakiabudu masanamu kama wao. Makafiri wakasema kuwaambia Waislamu, Wakristo watu wa Kitabu kama ninyi, wameshindwa na washirikina wenzetu, na hii ni alama ya kuwa karibuni na sisi tutawashindeni.

Qur'an ilitangaza Aya hizo zenye bishara mbili: Bishara ya kwanza ni kuwa katika muda wa miaka 9 Waajemi watashindwa *na siku hiyo waaminio watafurahi,* yaani makafiri wa Makka nao watashindwa.

Katika mwaka 624 Hirakla, mfalme wa Warumi aliingia Media katika nchi ya Ajemi na akalihilikisha hekalu la kuabudu moto la Goudzak (Enc. Br. Art. "Chosroes II"). Katika mwaka huo huo Waislamu 313 wasiojua kupigana, wanyonge, wenye silaha hafifu wakajikusuru kupambana na jeshi la makafiri 1,000 mastadi wa vita waliokuja kwa nia ya kuwaangamiza. Vita

بِنَصْرِ اللّٰهِ ؕ يَنْصُرُ مَنْ يَّشَآءُ ؕ وَهُوَ الْعَزِيْزُ الرَّحِيْمُ ۙ﴿۶﴾

6. Kwa msaada wa Allah; Humsaidia Amtakaye; naye ni Mshindi kamili, Mwenye rehema.

وَعْدَ اللّٰهِ ؕ لَا يُخْلِفُ اللّٰهُ وَعْدَهٗ وَلٰكِنَّ اَكْثَرَ النَّاسِ لَا يَعْلَمُوْنَ ﴿۷﴾

7. (Hii ni) ahadi ya Allah. Allah Havunji ahadi Yake, lakini watu wengi hawajui.

يَعْلَمُوْنَ ظَاهِرًا مِّنَ الْحَيٰوةِ الدُّنْيَا ۖ وَهُمْ عَنِ الْاٰخِرَةِ هُمْ غٰفِلُوْنَ ﴿۸﴾

8. Wanajua hali ya dhahiri ya maisha ya dunia, nao ndio wameghafilika na Akhera.

اَوَلَمْ يَتَفَكَّرُوْا فِيْۤ اَنْفُسِهِمْ ؕ مَا خَلَقَ اللّٰهُ السَّمٰوٰتِ وَالْاَرْضَ وَمَا بَيْنَهُمَاۤ اِلَّا بِالْحَقِّ وَاَجَلٍ مُّسَمًّى ؕ وَاِنَّ كَثِيْرًا مِّنَ النَّاسِ بِلِقَآئِ رَبِّهِمْ لَكٰفِرُوْنَ ﴿۹﴾

9. Je, hawatafakari nafsini mwao: Allah Hakuumba mbingu na ardhi na vilivyomo kati yao ila kwa haki na kwa muda uliowekwa? Na kwa yakini watu wengi wanakataa kukutana na Mola wao.

اَوَلَمْ يَسِيْرُوْا فِى الْاَرْضِ فَيَنْظُرُوْا كَيْفَ كَانَ عَاقِبَةُ الَّذِيْنَ مِنْ قَبْلِهِمْ ؕ كَانُوْۤا اَشَدَّ مِنْهُمْ قُوَّةً وَّاَثَارُوا الْاَرْضَ وَعَمَرُوْهَاۤ اَكْثَرَ مِمَّا عَمَرُوْهَا وَجَآءَتْهُمْ رُسُلُهُمْ بِالْبَيِّنٰتِ ؕ فَمَا كَانَ اللّٰهُ لِيَظْلِمَهُمْ وَلٰكِنْ كَانُوْۤا اَنْفُسَهُمْ يَظْلِمُوْنَ ﴿۱۰﴾

10. Je, hawatembei katika nchi na kuona jinsi ulivyokuwa mwisho wa wale waliokuwa kabla yao? wao walikuwa wenye nguvu zaidi kuliko hawa, na wakiilima ardhi na kuistawisha zaidi kuliko hawa walivyostawisha, na Mitume wao waliwafikia kwa dalili waziwazi, basi hakuwa Allah wa kuwadhulumu, lakini walikuwa wenyewe wakijidhulumu.

ثُمَّ كَانَ عَاقِبَةَ الَّذِيْنَ اَسَآءُوا السُّوْٓاٰۤى اَنْ كَذَّبُوْا بِاٰيٰتِ اللّٰهِ وَكَانُوْا بِهَا يَسْتَهْزِءُوْنَ ﴿۱۱﴾ ع

11. Kisha ulikuwa mbaya mwisho wa wale waliofanya ubaya kwa kuzikadhibisha Aya za Allah, na walikuwa wakizifanyia mzaha.

---

ikapiganwa katika mtaa wa Badri na makafiri wakashindwa vibaya. Hivyo bishara iliyotangazwa hapa ikatimia.

Aya hizi ziliposhuka makafiri walizibisha; basi Seyidna Abu Bakar akaweka dau la ngamia mia kwa mia na kafiri mmoja aitwaye Ubayya bin Khalf. Huyu Ubayya bin Khalf alikufa kabla ya tokeo hili, na Seyidna Abu Bakar alichukua ngamia kwa mrithi wake, na Mtume s.a.w. akamwambia azitoe sadaka (Baidhawi).

Padre Dale ameona husuda sana kutimia kwa bishara hii ya ajabu na hana asemalo isipokuwa ati ilikuwa ni kukisia, na anatoa mfano wa Waingereza na Wajerumani. Lakini kama ni kukisia iliwezekanaje Mtume kukisia kuwa wafuasi wake wawili watatu walio dhaifu baada ya miaka

FUNGU 2

اَللّٰهُ يَبْدَؤُا الْخَلْقَ ثُمَّ يُعِيْدُهٗ ثُمَّ اِلَيْهِ تُرْجَعُوْنَ ﴿١٢﴾

12. Allah Huanzisha kiumbe tena Hukirudisha mara ya pili, kisha mtarudishwa Kwake.

وَيَوْمَ تَقُوْمُ السَّاعَةُ يُبْلِسُ الْمُجْرِمُوْنَ ﴿١٣﴾

13. Na siku itakaposimama saa hiyo wakosefu watakata tamaa.

وَلَمْ يَكُنْ لَّهُمْ مِّنْ شُرَكَآئِهِمْ شُفَعٰٓؤُا وَكَانُوْا بِشُرَكَآئِهِمْ كٰفِرِيْنَ ﴿١٤﴾

14. (Watu) hawatakuwa na waombezi miongoni mwa washirika wao, nao watawakataa washirika wao.

وَيَوْمَ تَقُوْمُ السَّاعَةُ يَوْمَئِذٍ يَّتَفَرَّقُوْنَ ﴿١٥﴾

15. Na siku itakapotokea saa hiyo, basi siku hiyo, ndipo watafarakana.

فَاَمَّا الَّذِيْنَ اٰمَنُوْا وَعَمِلُوا الصّٰلِحٰتِ فَهُمْ فِيْ رَوْضَةٍ يُّحْبَرُوْنَ ﴿١٦﴾

16. Lakini wale walioamini na kutenda mema, basi wao watafurahishwa katika bustani.

وَاَمَّا الَّذِيْنَ كَفَرُوْا وَكَذَّبُوْا بِاٰيٰتِنَا وَلِقَآءِ الْاٰخِرَةِ فَاُولٰٓئِكَ فِي الْعَذَابِ مُحْضَرُوْنَ ﴿١٧﴾

17. Na waliokufuru na wakazikadhibisha Aya Zetu na mkutano wa Akhera, basi hao watahudhurishwa katika adhabu.

فَسُبْحٰنَ اللّٰهِ حِيْنَ تُمْسُوْنَ وَحِيْنَ تُصْبِحُوْنَ ﴿١٨﴾

18. Basi Mtukuzeni Allah mnapouingia usiku na mnapoiingia asubuhi.

وَلَهُ الْحَمْدُ فِي السَّمٰوٰتِ وَالْاَرْضِ وَعَشِيًّا وَّحِيْنَ تُظْهِرُوْنَ ﴿١٩﴾

19. Na sifa zote njema ni Zake mbinguni na ardhini, na wakati wa alasiri na mnapoingia adhuhuri.

يُخْرِجُ الْحَيَّ مِنَ الْمَيِّتِ وَيُخْرِجُ الْمَيِّتَ مِنَ الْحَيِّ وَيُحْيِ الْاَرْضَ بَعْدَ مَوْتِهَا ؕ وَكَذٰلِكَ تُخْرَجُوْنَ ﴿٢٠﴾ ع

20. Hukitoa kilicho hai katika kilichokufa, na Hukitoa kilichokufa katika kilicho hai, na Huihuisha ardhi baada ya kufa kwake. Na hivyo ndivyo mtakavyotolewa.

---

kumi watawashinda makafiri wenye nguvu kabisa? Angewezaje kukisia kuwa ufalme uliovunjwa kabisa wa Kirumi katika muda barabara wa miaka 9 utajilipiza na kumshinda adui yao hali hana habari watainuka namna gani? Mtume angekuwa mwongo Mungu Angemfedhehesha hapa, maana kukisia kwa mtu hivi hivi ni mbali na kwa mtu ambaye kukisia kwake kunaweza kuwapoteza watu waangamie kama kukitokea sawasawa.

Aya 18 - 19. Ibni Abbas anasema ya kwamba hapa sala tano zimeelezwa: *Hiina tumsuun* (mnapouingia usiku) ni Sala ya Magharibi na Isha. *Hiina tusbihuun* (mnapoiingia asubuhi) ni Sala ya Alfajiri. Ashiyyan (wakati wa alasiri ni Sala ya Asri. *Hiina tudh-hiruun* (mnapoiingia adhuhuri) ni Sala ya Adhuhuri (Baidhawi).

FUNGU 3

وَمِنْ اٰيٰتِهٖۤ اَنْ خَلَقَكُمْ مِّنْ تُرَابٍ ثُمَّ اِذَاۤ اَنْتُمْ بَشَرٌ تَنْتَشِرُوْنَ ﴿٢١﴾

21. Na katika Ishara Zake ni hii ya kwamba Amewaumbeni kwa udongo, kisha mmekuwa watu mnaoenea.

وَمِنْ اٰيٰتِهٖۤ اَنْ خَلَقَ لَكُمْ مِّنْ اَنْفُسِكُمْ اَزْوَاجًا لِّتَسْكُنُوْۤا اِلَيْهَا وَجَعَلَ بَيْنَكُمْ مَّوَدَّةً وَّ رَحْمَةً ؕ اِنَّ فِيْ ذٰلِكَ لَاٰيٰتٍ لِّقَوْمٍ يَّتَفَكَّرُوْنَ ﴿٢٢﴾

22. Na katika Ishara Zake ni kuwa Amewaumbieni katika jinsi yenu wake ili mpate utulivu kwao, naye Amejaalia mapenzi na huruma baina yenu. Bila shaka katika hayo zimo Ishara kwa watu wanaotafakari.

وَمِنْ اٰيٰتِهٖ خَلْقُ السَّمٰوٰتِ وَالْاَرْضِ وَاخْتِلَافُ اَلْسِنَتِكُمْ وَ اَلْوَانِكُمْ ؕ اِنَّ فِيْ ذٰلِكَ لَاٰيٰتٍ لِّلْعٰلِمِيْنَ ﴿٢٣﴾

23. Na katika Ishara Zake ni umbo la mbingu na ardhi, na hitilafu ya lugha zenu na rangi zenu. Kwa yakini katika hayo zimo Ishara kwa wenye elimu.

وَمِنْ اٰيٰتِهٖ مَنَامُكُمْ بِالَّيْلِ وَ النَّهَارِ وَابْتِغَآؤُكُمْ مِّنْ فَضْلِهٖ ؕ اِنَّ فِيْ ذٰلِكَ لَاٰيٰتٍ لِّقَوْمٍ يَّسْمَعُوْنَ ﴿٢٤﴾

24. Na katika Ishara Zake ni kulala kwenu kwa usiku na mchana, na (pia) kutafuta kwenu fadhili Yake. Hakika katika hayo zimo Ishara kwa watu wanaosikia.

وَمِنْ اٰيٰتِهٖ يُرِيْكُمُ الْبَرْقَ خَوْفًا وَّطَمَعًا وَّيُنَزِّلُ مِنَ السَّمَآءِ مَآءً فَيُحْيٖ بِهِ الْاَرْضَ بَعْدَ مَوْتِهَا ؕ اِنَّ فِيْ ذٰلِكَ لَاٰيٰتٍ لِّقَوْمٍ يَّعْقِلُوْنَ ﴿٢٥﴾

25. Na katika Ishara Zake ni kuwaonyesheni umeme kwa hofu na tumaini, na kuteremsha maji kutoka mawinguni, kwayo Huifufua ardhi baada ya kufa kwake. Bila shaka katika hayo zimo Ishara kwa watu wanaofahamu.

وَمِنْ اٰيٰتِهٖۤ اَنْ تَقُوْمَ السَّمَآءُ وَ الْاَرْضُ بِاَمْرِهٖ ؕ ثُمَّ اِذَا دَعَاكُمْ دَعْوَةً ۖ مِّنَ الْاَرْضِ ۖ اِذَاۤ اَنْتُمْ تَخْرُجُوْنَ ﴿٢٦﴾

26. Na katika Ishara Zake ni kuwa mbingu na ardhi husimama kwa amri Yake; kisha Atakapowaiteni wito mmoja, nanyi ndipo mtatoka ardhini.

وَلَهٗ مَنْ فِي السَّمٰوٰتِ وَ الْاَرْضِ ؕ كُلٌّ لَّهٗ قٰنِتُوْنَ ﴿٢٧﴾

27. Vilivyomo mbinguni na ardhini ni Vyake, vyote humtii.

وَهُوَ الَّذِيْ يَبْدَؤُا الْخَلْقَ ثُمَّ يُعِيْدُهٗ وَهُوَ اَهْوَنُ عَلَيْهِ ؕ وَلَهُ الْمَثَلُ الْاَعْلٰى فِي السَّمٰوٰتِ وَالْاَرْضِ ۚ وَ هُوَ الْعَزِيْزُ الْحَكِيْمُ ﴿٢٨﴾ ع

28. Na Yeye ndiye Anayeanzisha kiumbe na ndiye Atakayekirudisha mara nyingine, na jambo hili ni rahisi Kwake; na sifa zilizotukuka katika mbingu na ardhi ni Zake, naye ndiye Mwenye nguvu, Mwenye hekima.

Aya 23. *Hitilafu ya lugha zenu na rangi zenu.* Kama vile mbingu na ardhi

FUNGU 4

ضَرَبَ لَكُمْ مَّثَلًا مِّنْ اَنْفُسِكُمْ ؕ هَلْ
لَّكُمْ مِّنْ مَّا مَلَكَتْ اَيْمَانُكُمْ مِّنْ شُرَكَآءَ
فِيْ مَا رَزَقْنٰكُمْ فَاَنْتُمْ فِيْهِ سَوَآءٌ
تَخَافُوْنَهُمْ كَخِيْفَتِكُمْ اَنْفُسَكُمْ ؕ كَذٰلِكَ
نُفَصِّلُ الْاٰيٰتِ لِقَوْمٍ يَّعْقِلُوْنَ ﴿۲۹﴾

29. Amewapigieni mfano kwa hali ya nafsi zenu; je, katika hao iliyowatamalaki mikono yenu ya kuume kuna washirika wenu katika yale Tuliyowapeni hata mkashiriki sawasawa, mkawaogopa kama mnavyoogopana wenyewe? Hivyo ndivyo Tuelezavyo Ishara kwa watu wanaofahamu.

بَلِ اتَّبَعَ الَّذِيْنَ ظَلَمُوْٓا اَهْوَآءَهُمْ
بِغَيْرِ عِلْمٍ ۚ فَمَنْ يَّهْدِيْ مَنْ اَضَلَّ اللّٰهُ ؕ
وَمَا لَهُمْ مِّنْ نّٰصِرِيْنَ ﴿۳۰﴾

30. Lakini waliodhulumu waliyafuata matamanio yao pasipo kujua; basi ni nani awezaye kumwogoza ambaye Allah Amemwacha kupotea? Nao hawatakuwa na wasaidizi.

فَاَقِمْ وَجْهَكَ لِلدِّيْنِ حَنِيْفًا ؕ فِطْرَتَ
اللّٰهِ الَّتِيْ فَطَرَ النَّاسَ عَلَيْهَا ؕ لَا تَبْدِيْلَ
لِخَلْقِ اللّٰهِ ؕ ذٰلِكَ الدِّيْنُ الْقَيِّمُ ۙ وَلٰكِنَّ
اَكْثَرَ النَّاسِ لَا يَعْلَمُوْنَ ۙ﴿۳۱﴾

31. Basi uelekeze uso wako kwenye dini ukiwa daima umeegemea kwenye haki - hii ni asili ya Allah ambayo kwayo Aliwaumba binadamu wote. Hakuna mabadiliko katika uumbaji wa Allah. Bila shaka hiyo ndiyo dini iliyosimama madhubuti na inazisaidia zingine kusimama wima. Lakini watu wengi hawajui.

---

zinaonyesha uwezo wa Allah, namna hii rangi na lugha mbalimbali za watu zinaonyesha uwezo wa Mwenyezi Mungu, siyo kwamba ziwe sababu ya watu kuchukiana na kubughudhiana.

Aya 31. *Ndilo umbile la Allah alilowaumbia watu.* Dini ya Kiislamu inatoa mafundisho yaliyo sawa kabisa na asili ya mwanadamu. Mafundisho yake juu ya Umoja wa Allah, na kufika kwa ufunuo kila upande wa dunia, na kupata malipo ya vitendo, ni mambo yanayokubaliwa na mataifa yote. Hata huwezi kukuta fundisho lo lote la kishenzi au lililo kinyume na ustaarabu hasa katika Uislamu. Mtume *s.a.w.* alisema, "Hakuna azaliwaye ila anazaliwa juu ya kawaida ya asili ambayo ni Uislamu, lakini wazazi wake wanamfanya Myahudi au Mkristo au Mmajusi; kama vile mnyama anazaliwa mnyama kamili katika viungo vyake, je mmepata kumwona na ulema?" (Bukhari).

Hapa hali asilia ya Allah ina maana ya sifa Zake. Katika maudhui hii ina maana kwamba mtu amepewa uwezo wa kuziigiza sifa za Allah. Hiyo ndiyo njia pekee ambayo kwayo mtu anaweza kupata mageuzi ya kiroho. Ni dhahiri kwamba wanyama wengine hawawezi kuwa na hisa katika hali hii pekee ya binadamu. Yaani kumkaribia Allah

مُنِيْبِيْنَ اِلَيْهِ وَاتَّقُوْهُ وَاَقِيْمُوا الصَّلٰوةَ
وَلَا تَكُوْنُوْا مِنَ الْمُشْرِكِيْنَ ﴿٣٢﴾

32. Nyenyekeeni Kwake na Mcheni, na simamisheni Sala, wala msiwe katika washirikina,

مِنَ الَّذِيْنَ فَرَّقُوْا دِيْنَهُمْ وَكَانُوْا شِيَعًا ؕ
كُلُّ حِزْبٍۢ بِمَا لَدَيْهِمْ فَرِحُوْنَ ﴿٣٣﴾

33. Katika wale waliotenga dini yao wakawa makundi-makundi; kila kundi hufurahia waliyo nayo.

وَاِذَا مَسَّ النَّاسَ ضُرٌّ دَعَوْا رَبَّهُمْ
مُّنِيْبِيْنَ اِلَيْهِ ثُمَّ اِذَآ اَذَاقَهُمْ مِّنْهُ رَحْمَةً
اِذَا فَرِيْقٌ مِّنْهُمْ بِرَبِّهِمْ يُشْرِكُوْنَ ﴿٣٤﴾

34. Na udhia unapowashika watu, humwomba Mola wao kwa kunyenyekea, kisha Anapowaonjesha rehema Yake, hapo kundi moja miongoni mwao mara humshirikisha Mola wao,

لِيَكْفُرُوْا بِمَآ اٰتَيْنٰهُمْ ؕ فَتَمَتَّعُوْا ۟
فَسَوْفَ تَعْلَمُوْنَ ﴿٣٥﴾

35. Kwa kuyakataa Tuliyowapa, basi jinufaisheni kwa muda, basi karibuni mtajua.

اَمْ اَنْزَلْنَا عَلَيْهِمْ سُلْطٰنًا فَهُوَ يَتَكَلَّمُ بِمَا
كَانُوْا بِهٖ يُشْرِكُوْنَ ﴿٣٦﴾

36. Je, Tumewataremshia dalili inayowaambia juu ya yale wamshirikishayo nayo?

وَاِذَآ اَذَقْنَا النَّاسَ رَحْمَةً فَرِحُوْا بِهَا ؕ وَاِنْ
تُصِبْهُمْ سَيِّئَةٌ ۢ بِمَا قَدَّمَتْ اَيْدِيْهِمْ
اِذَا هُمْ يَقْنَطُوْنَ ﴿٣٧﴾

37. Na Tunapowaonjesha watu rehema, huifurahia, na kama ukiwafikia ubaya kwa sababu ya yale iliyoyatanguliza mikono yao, mara wanakata tamaa.

اَوَلَمْ يَرَوْا اَنَّ اللّٰهَ يَبْسُطُ الرِّزْقَ لِمَنْ
يَّشَآءُ وَيَقْدِرُ ؕ اِنَّ فِيْ ذٰلِكَ لَاٰيٰتٍ لِّقَوْمٍ
يُّؤْمِنُوْنَ ﴿٣٨﴾

38. Je, hawaoni ya kwamba Allah Hutoa riziki nyingi kwa Amtakaye na Hudhikisha? Bila shaka katika hayo zimo Ishara kwa watu wanaoamini.

فَاٰتِ ذَا الْقُرْبٰى حَقَّهٗ وَالْمِسْكِيْنَ وَابْنَ
السَّبِيْلِ ؕ ذٰلِكَ خَيْرٌ لِّلَّذِيْنَ يُرِيْدُوْنَ
وَجْهَ اللّٰهِ ۫ وَاُولٰٓئِكَ هُمُ الْمُفْلِحُوْنَ ﴿٣٩﴾

39. Basi mpe ndugu haki yake na maskini, na msafiri. Hayo ni bora kwa wale wanaotaka radhi ya Allah; na hao ndio wenye kufaulu.

---

kwaweza kupatikana tu iwapo sifa Zake zilizo bora zitaigizwa. Lakini ni lazima ikumbukwe kwamba Allah hana mwisho ambapo binadamu ana mwisho. Hivyo basi binadamu anaweza kumuigiza Yeye ndani ya ukomo wa kibinadamu.

Aya 39. *Haki yake*. Mtu anapotoa kuwapa jamaa na ndugu cho chote, basi ajue ya kuwa namna hii anatimiza wajibu wake na anatoa haki zao zilizo katika mali na vifaa vyake.

وَمَآ اٰتَيْتُمْ مِّنْ رِّبًا لِّيَرْبُوَا۟ فِىْٓ اَمْوَالِ
النَّاسِ فَلَا يَرْبُوْا عِنْدَ اللّٰهِ ۚ وَمَآ اٰتَيْتُمْ
مِّنْ زَكٰوةٍ تُرِيْدُوْنَ وَجْهَ اللّٰهِ فَاُولٰٓئِكَ
هُمُ الْمُضْعِفُوْنَ ﴿٣٩﴾

40. Na riba ile mtoayo ili izidi katika mali ya watu, basi mbele ya Allah haizidi; lakini (mali) mnayoitoa Zaka kwa kutaka radhi ya Allah, basi hao ndio wazidishao (mali zao).

اَللّٰهُ الَّذِىْ خَلَقَكُمْ ثُمَّ رَزَقَكُمْ ثُمَّ
يُمِيْتُكُمْ ثُمَّ يُحْيِيْكُمْ ؕ هَلْ مِنْ
شُرَكَآئِكُمْ مَّنْ يَّفْعَلُ مِنْ ذٰلِكُمْ مِّنْ
شَىْءٍ ؕ سُبْحٰنَهٗ وَتَعٰلٰى عَمَّا يُشْرِكُوْنَ ﴿٤٠﴾ ع

41. Allah ndiye Aliyewaumbeni, kisha Akawapeni riziki, kisha Atawafisheni, kisha Atawafufueni. Je, miongoni mwa washirika wenu yuko awezaye kufanya lo lote katika hayo? Yeye Ameepukana na upungufu, na Yu juu kabisa kuliko yale wanayomshirikisha nayo.

FUNGU 5

ظَهَرَ الْفَسَادُ فِى الْبَرِّ وَالْبَحْرِ بِمَا كَسَبَتْ
اَيْدِى النَّاسِ لِيُذِيْقَهُمْ بَعْضَ الَّذِىْ
عَمِلُوْا لَعَلَّهُمْ يَرْجِعُوْنَ ﴿٤١﴾

42. Ufisadi umedhihirika barani na baharini kwa sababu ya yale iliyoyafanya mikono ya watu, ili Awaonjeshe (adhabu ya) sehemu ya waliyoyafanya, huenda warudie.

قُلْ سِيْرُوْا فِى الْاَرْضِ فَانْظُرُوْا كَيْفَ
كَانَ عَاقِبَةُ الَّذِيْنَ مِنْ قَبْلُ ؕ
كَانَ اَكْثَرُهُمْ مُّشْرِكِيْنَ ﴿٤٢﴾

43. Sema: Safirini ardhini na tazameni jinsi ulivyokuwa mwisho wa wale waliotangulia, wengi wao walikuwa washirikina.

فَاَقِمْ وَجْهَكَ لِلدِّيْنِ الْقَيِّمِ مِنْ قَبْلِ اَنْ
يَّاْتِىَ يَوْمٌ لَّا مَرَدَّ لَهٗ مِنَ اللّٰهِ يَوْمَئِذٍ
يَّصَّدَّعُوْنَ ﴿٤٣﴾

44. Basi elekeza uso wako kwenye dini iliyo madhubuti na yenye kudumu, kabla ya kufika kwa siku isiyozuilika kutoka kwa Allah. Siku hiyo watatengana.

Aya 40. Watu wanaotoa au kupokea riba wajue ya kuwa ingawa wanaweza kujiongezea faida ya dunia hii lakini kwa Allah wao watakuwa na hasara kabisa na maangamizo ya namna-namna yanayoweza kuwafikia wao au wazao wao. Katika sura 2:280 imehadharishwa ya kuwa riba isipoachwa italeta vita.

Aya 42. Aya hii inashuhudiwa na historia ya kuwa alipofika Mtume *s.a.w.* ulimwengu

مَنْ كَفَرَ فَعَلَيْهِ كُفْرُهٗ ۚ وَمَنْ عَمِلَ صَالِحًا فَلِاَنْفُسِهِمْ يَمْهَدُوْنَ ﴿٤٥﴾

45. Anayekufuru, basi (madhara ya) kufuru yake ni juu yake; na afanyaye mema, basi (hao) wanazitengenezea nafsi zao,

لِيَجْزِيَ الَّذِيْنَ اٰمَنُوْا وَعَمِلُوا الصّٰلِحٰتِ مِنْ فَضْلِهٖ ۭ اِنَّهٗ لَا يُحِبُّ الْكٰفِرِيْنَ ﴿٤٦﴾

46. Ili Awalipe wale walioamini na kufanya vitendo vizuri katika fadhili Yake. Bila shaka Yeye Hawapendi makafiri.

وَمِنْ اٰيٰتِهٖٓ اَنْ يُّرْسِلَ الرِّيَاحَ مُبَشِّرٰتٍ وَّلِيُذِيْقَكُمْ مِّنْ رَّحْمَتِهٖ وَلِتَجْرِيَ الْفُلْكُ بِاَمْرِهٖ وَلِتَبْتَغُوْا مِنْ فَضْلِهٖ وَلَعَلَّكُمْ تَشْكُرُوْنَ ﴿٤٧﴾

47. Na katika Ishara Zake ni kuzituma pepo ziletazo habari nzuri, na ili kuwaonjesheni rehema Yake, na ili zitembee merikebu kwa amri Yake, na mzitafute fadhili Zake, na ili mtoe shukurani.

وَلَقَدْ اَرْسَلْنَا مِنْ قَبْلِكَ رُسُلًا اِلٰى قَوْمِهِمْ فَجَآءُوْهُمْ بِالْبَيِّنٰتِ فَانْتَقَمْنَا مِنَ الَّذِيْنَ اَجْرَمُوْا ۭ وَكَانَ حَقًّا عَلَيْنَا نَصْرُ الْمُؤْمِنِيْنَ ﴿٤٨﴾

48. Na Kwa hakika Tuliwatuma kabla yako Mitume kwa watu wao, na wakaawafikia kwa Ishara waziwazi, kisha Tukawaadhibu wale waliokosa, na ilikuwa haki juu Yetu kuwasaidia waaminio.

اَللّٰهُ الَّذِيْ يُرْسِلُ الرِّيٰحَ فَتُثِيْرُ سَحَابًا فَيَبْسُطُهٗ فِي السَّمَاۗءِ كَيْفَ يَشَاۗءُ وَيَجْعَلُهٗ كِسَفًا فَتَرَى الْوَدْقَ يَخْرُجُ مِنْ خِلٰلِهٖ ۚ فَاِذَآ اَصَابَ بِهٖ مَنْ يَّشَاۗءُ مِنْ عِبَادِهٖٓ اِذَا هُمْ يَسْتَبْشِرُوْنَ ﴿٤٩﴾

49. Allah ndiye Anayezituma pepo ndipo zinainua mawingu, kisha Anayatandaza mbinguni kama Apendavyo, na Anayafanya vipande vipande, kisha unaona mvua ikitoka ndani yake; na Anapoifikisha kwa Amtakaye katika watumishi Wake, mara wanafurahi,

وَاِنْ كَانُوْا مِنْ قَبْلِ اَنْ يُّنَزَّلَ عَلَيْهِمْ مِّنْ قَبْلِهٖ لَمُبْلِسِيْنَ ﴿٥٠﴾

50. Na ingawa kabla ya kuwateremshia walikuwa wenye kukata tamaa.

فَانْظُرْ اِلٰٓى اٰثٰرِ رَحْمَتِ اللّٰهِ كَيْفَ يُحْيِ الْاَرْضَ بَعْدَ مَوْتِهَا ۭ اِنَّ ذٰلِكَ لَمُحْيِ الْمَوْتٰى ۚ وَهُوَ عَلٰي كُلِّ شَيْءٍ قَدِيْرٌ ﴿٥١﴾

51. Basi ziangalie alama za rehema za Allah, jinsi Anavyoihuisha ardhi baada ya kufa kwake; bila shaka Yeye ndiye Mwenye kuhuisha wafu: Naye ndiye Mwenye uwezo juu ya kila kitu.

mzima ulikuwa katika giza na ufisadi. Ukristo nao, asemavyo Sir William Muir, ulikuwa umelemaa na kuharibika.

وَلَئِنْ اَرْسَلْنَا رِيْحًا فَرَاَوْهُ مُصْفَرًّا لَّظَلُّوْا مِنْۢ بَعْدِهٖ يَكْفُرُوْنَ ﴿٥٢﴾

52. Na kama Tukiutuma upepo na wakauona umekuwa rangi ya manjano, juu ya hayo kwa yakini wataendelea kukufuru.

فَاِنَّكَ لَا تُسْمِعُ الْمَوْتٰى وَلَا تُسْمِعُ الصُّمَّ الدُّعَآءَ اِذَا وَلَّوْا مُدْبِرِيْنَ ﴿٥٣﴾

53. Na wewe, bila shaka, huwezi kuwasikilizisha wafu, wala huwezi kuwasikilizisha viziwi wito, watakapogeuka kurudi nyuma.

وَمَآ اَنْتَ بِهٰدِ الْعُمْيِ عَنْ ضَلٰلَتِهِمْ ؕ اِنْ تُسْمِعُ اِلَّا مَنْ يُّؤْمِنُ بِاٰيٰتِنَا فَهُمْ مُّسْلِمُوْنَ ﴿٥٤﴾ ع

54. Wala huwezi kuwaongoza vipofu katika upotevu wao. Huwasikilizishi ila wanaoziamini Aya Zetu, kisha wanakuwa watii.

FUNGU 6

اَللّٰهُ الَّذِيْ خَلَقَكُمْ مِّنْ ضُعْفٍ ثُمَّ جَعَلَ مِنْۢ بَعْدِ ضُعْفٍ قُوَّةً ثُمَّ جَعَلَ مِنْۢ بَعْدِ قُوَّةٍ ضُعْفًا وَّشَيْبَةً ؕ يَخْلُقُ مَا يَشَآءُ ۚ وَهُوَ الْعَلِيْمُ الْقَدِيْرُ ﴿٥٥﴾

55. Allah ndiye Aliyewaumbeni katika udhaifu, na baada ya udhaifu Akafanya nguvu, kisha baada ya nguvu Akaufanya udhaifu na uzee; Huumba Apendavyo; naye ni Mjuzi, Mwenye uwezo.

وَيَوْمَ تَقُوْمُ السَّاعَةُ يُقْسِمُ الْمُجْرِمُوْنَ ۙ مَا لَبِثُوْا غَيْرَ سَاعَةٍ ؕ كَذٰلِكَ كَانُوْا يُؤْفَكُوْنَ ﴿٥٦﴾

56. Na siku itakaposimama saa ile, wakosefu wataapa (ya kwamba) hawakukaa isipokuwa saa moja tu. Hivyo ndivyo walivyokuwa wakigeuzwa.

وَقَالَ الَّذِيْنَ اُوْتُوا الْعِلْمَ وَالْاِيْمَانَ لَقَدْ لَبِثْتُمْ فِيْ كِتٰبِ اللّٰهِ اِلٰى يَوْمِ الْبَعْثِ ۚ فَهٰذَا يَوْمُ الْبَعْثِ وَلٰكِنَّكُمْ كُنْتُمْ لَا تَعْلَمُوْنَ ﴿٥٧﴾

57. Na waliopewa elimu na imani watasema: Hakika ninyi mmekaa kwa hukumu ya Allah mpaka siku ya ufufuo, basi hii ni siku ya ufufuo, lakini ninyi mlikuwa hamjui.

فَيَوْمَئِذٍ لَّا يَنْفَعُ الَّذِيْنَ ظَلَمُوْا مَعْذِرَتُهُمْ وَلَا هُمْ يُسْتَعْتَبُوْنَ ﴿٥٨﴾

58. Na siku hiyo hautawafaa waliodhulumu udhuru wao, wala hawatapewa fursa ya kukifikia kizingiti Chake.

وَلَقَدْ ضَرَبْنَا لِلنَّاسِ فِيْ هٰذَا الْقُرْاٰنِ مِنْ كُلِّ مَثَلٍ ؕ وَلَئِنْ جِئْتَهُمْ بِاٰيَةٍ لَّيَقُوْلَنَّ الَّذِيْنَ كَفَرُوْٓا اِنْ اَنْتُمْ اِلَّا مُبْطِلُوْنَ ﴿٥٨﴾

59. Na kwa yakini Tumepiga mfano wa kila namna kwa ajili ya watu katika Qur'an hii. Na kama ukiwafikia na Ishara, bila shaka wale waliokufuru watasema: Ninyi si cho chote ila mshikao batili.

كَذٰلِكَ يَطْبَعُ اللّٰهُ عَلٰى قُلُوْبِ الَّذِيْنَ لَا يَعْلَمُوْنَ ﴿٥٩﴾

60. Hivi ndivyo Allah Hupiga muhuri mioyoni mwa wale wasio na elimu.

فَاصْبِرْ اِنَّ وَعْدَ اللّٰهِ حَقٌّ وَّلَا يَسْتَخِفَّنَّكَ الَّذِيْنَ لَا يُوْقِنُوْنَ ﴿٦٠﴾ ع ٧

61. Basi subiri, bila shaka ahadi ya Allah ni haki, wala wasikuhafifishe wale wasiokuwa na yakini.

سُوْرَةُ لُقْمَانَ مَكِّيَّةٌ وَّ هِيَ مَعَ الْبَسْمَلَةِ خَمْسٌ وَّ ثَلَاثُوْنَ اٰيَةً وَّ اَرْبَعَةُ رُكُوْعَاتٍ

31. SURA LUQMAAN

Imeteremshwa Makka

Ina mafungu 4 na Aya 35 pamoja na Bismillahi.

بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ ①

1. Kwa jina la Allah, Mwingi wa rehema, Mwingi wa ukarimu.

الٓمّٓ ②

2. Mimi ni Allah Nijuaye sana.

تِلْكَ اٰيٰتُ الْكِتٰبِ الْحَكِيْمِ ③

3. Hizi ndizo Aya za Kitabu chenye hekima,

هُدًى وَّ رَحْمَةً لِّلْمُحْسِنِيْنَ ④

4. Mwongozo na rehema kwa wafanyao wema.

الَّذِيْنَ يُقِيْمُوْنَ الصَّلٰوةَ وَ يُؤْتُوْنَ الزَّكٰوةَ وَ هُمْ بِالْاٰخِرَةِ هُمْ يُوْقِنُوْنَ ⑤

5. Wale wanaosimamisha Sala na kutoa Zaka, na ambao wana yakini na Akhera,

اُولٰٓئِكَ عَلٰى هُدًى مِّنْ رَّبِّهِمْ وَ اُولٰٓئِكَ هُمُ الْمُفْلِحُوْنَ ⑥

6. Hao ndio wako juu ya mwongozo utokao kwa Mola wao, na hao ndio wenye kufaulu.

وَ مِنَ النَّاسِ مَنْ يَّشْتَرِيْ لَهْوَ الْحَدِيْثِ لِيُضِلَّ عَنْ سَبِيْلِ اللّٰهِ بِغَيْرِ عِلْمٍ ۖ وَّ يَتَّخِذَهَا هُزُوًا ؕ اُولٰٓئِكَ لَهُمْ عَذَابٌ مُّهِيْنٌ ⑦

7. Na katika watu yupo anayenunua maneno ya upuuzi ili kupoteza katika njia ya Allah pasipo elimu, na kuifanyia mzaha. Hao watapata adhabu ifedheheshayo.

وَ اِذَا تُتْلٰى عَلَيْهِ اٰيٰتُنَا وَلّٰى مُسْتَكْبِرًا كَاَنْ لَّمْ يَسْمَعْهَا كَاَنَّ فِيْۤ اُذُنَيْهِ وَقْرًا ۚ فَبَشِّرْهُ بِعَذَابٍ اَلِيْمٍ ⑧

8. Na anaposomewa Aya Zetu, hurudi kwa kujivuna kama hakuzisikia, kana kwamba masikioni mwake mna uzito; basi mpe habari za adhabu iumizayo.

Jina la sura hii ni Seyidna Lukman mcha Mungu mkubwa aliyekuwa katika nchi ya ethiopia (Uhabeshi). Sura hii kadhalika ilishuka Makka ingawa baadhi ya watu wamehitilafiana: wengine wanasema baadhi ya Aya zake, na wengine sehemu yake kubwa, ndiyo ilishuka Madina.

Aya 2. *Alif Laam Miim* (Tazama sura 2:2).

Aya 7. *Anayenunua,* maana yake anayeshika.

إِنَّ الَّذِينَ آمَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ لَهُمْ
جَنَّاتُ النَّعِيمِ ﴿٩﴾

9. Bila shaka wale walioamini na wakafanya vitendo vizuri, zitakuwa kwao bustani za neema.

خَالِدِينَ فِيهَا ۖ وَعْدَ اللَّهِ حَقًّا ۚ وَهُوَ
الْعَزِيزُ الْحَكِيمُ ﴿١٠﴾

10. Watakaa humo - ni ahadi ya Allah iliyo haki, na Yeye Ndiye Mshindi kamili, Mwenye hekima.

خَلَقَ السَّمَاوَاتِ بِغَيْرِ عَمَدٍ تَرَوْنَهَا وَأَلْقَىٰ
فِي الْأَرْضِ رَوَاسِيَ أَنْ تَمِيدَ بِكُمْ وَبَثَّ
فِيهَا مِنْ كُلِّ دَابَّةٍ ۚ وَأَنْزَلْنَا مِنَ السَّمَاءِ مَاءً
فَأَنْبَتْنَا فِيهَا مِنْ كُلِّ زَوْجٍ كَرِيمٍ ﴿١١﴾

11. Ameziumba mbingu pasipo nguzo mzionazo; na Ameiweka milima ardhini ili (ardhi) isisukesuke nanyi; naye Ametawanya humo wanyama wa kila namna; na Tumeyateremsha maji kutoka mawinguni na humo Tumemeesha (mimea) mizuri ya kila aina.

هَٰذَا خَلْقُ اللَّهِ فَأَرُونِي مَاذَا خَلَقَ
الَّذِينَ مِنْ دُونِهِ ۚ بَلِ الظَّالِمُونَ
فِي ضَلَالٍ مُبِينٍ ﴿١٢﴾ ع

12. Huu ndio uumbaji wa Allah, basi Nionyesheni ni nini walichoumba wale walio kinyume naye. Bali wadhalimu wamo katika upotevu wa dhahiri

FUNGU 2

وَلَقَدْ آتَيْنَا لُقْمَانَ الْحِكْمَةَ أَنِ اشْكُرْ لِلَّهِ ۚ
وَمَنْ يَشْكُرْ فَإِنَّمَا يَشْكُرُ لِنَفْسِهِ ۖ
وَمَنْ كَفَرَ فَإِنَّ اللَّهَ غَنِيٌّ حَمِيدٌ ﴿١٣﴾

13. Na kwa yakini Tulimpa Lukmani hekima ya kwamba umshukuru Allah, na anayeshukuru, basi kwa yakini anashukuru kwa ajili ya nafsi yake; na anayekufuru, basi Allah ni Mkwasi, Asifiwaye.

وَإِذْ قَالَ لُقْمَانُ لِابْنِهِ وَهُوَ يَعِظُهُ
يَا بُنَيَّ لَا تُشْرِكْ بِاللَّهِ ۖ إِنَّ الشِّرْكَ
لَظُلْمٌ عَظِيمٌ ﴿١٤﴾

14. Na (kumbukeni) Lukmani alipomwambia mwanawe huku akimsihi: Ewe mwanangu, usimshirikishe Allah, hakika shirki ndiyo dhuluma kubwa.

Aya 11. *Antamiida bikum.* Maneno haya tumeyafasiri, "Ili isisukesuke nanyi." Pia maana yake ni "Ili iwape matumizi" na "ili msiangamie."

Aya 12. Allah anasema viumbe vyote hivi ni Vyake, na anasema wanaowaabudu miungu wengine waonyeshe miungu hao wameumba nini. Wakristo ilikuwa mahali pao wajute juu ya hoja hii nzito; lakini bila kumwogopa Allah wameanza kudai kuwa sisi wote pamoja na vitu vyote na viumbe vyote tuliumbwa na Yesu. Siyo madai ya bure haya? Yesu aliishi miaka mingi pamoja nao je wanaweza kutuambia aliumba kitu gani kipya ili kuhakikisha kuwa viumbe vilivyopo aliviumba yeye?

وَوَصَّيْنَا الْاِنْسَانَ بِوَالِدَيْهِ ۚ حَمَلَتْهُ اُمُّهٗ وَهْنًا عَلٰى وَهْنٍ وَّ فِصٰلُهٗ فِىْ عَامَيْنِ اَنِ اشْكُرْ لِىْ وَلِوَالِدَيْكَ ؕ اِلَىَّ الْمَصِيْرُ ﴿۱۵﴾

15. Na Tumemwusia mwanadamu kwa ajili ya wazazi wake - mama yake amembeba kwa udhaifu juu ya udhaifu, na kumwachisha kunyonya katika miaka miwili - ya kwamba unishukuru Mimi na wazazi wako; marudio (ya mwisho) ni Kwangu.

وَاِنْ جَاهَدٰكَ عَلٰٓى اَنْ تُشْرِكَ بِىْ مَا لَيْسَ لَكَ بِهٖ عِلْمٌ فَلَا تُطِعْهُمَا وَصَاحِبْهُمَا فِى الدُّنْيَا مَعْرُوْفًا ۖ وَّ اتَّبِعْ سَبِيْلَ مَنْ اَنَابَ اِلَىَّ ۚ ثُمَّ اِلَىَّ مَرْجِعُكُمْ فَاُنَبِّئُكُمْ بِمَا كُنْتُمْ تَعْمَلُوْنَ ﴿۱۶﴾

16. Na kama (wazazi wako) wakushurutishe kunishirikisha na (yule) ambaye huna habari naye, basi usiwatii; na usuhubiane nao duniani kwa wema; na shika njia ya yule anayeelekea Kwangu, kisha mtarejea Kwangu, basi Nitawaambieni mliyokuwa mkitenda.

يٰبُنَىَّ اِنَّهَآ اِنْ تَكُ مِثْقَالَ حَبَّةٍ مِّنْ خَرْدَلٍ فَتَكُنْ فِىْ صَخْرَةٍ اَوْ فِى السَّمٰوٰتِ اَوْ فِى الْاَرْضِ يَاْتِ بِهَا اللّٰهُ ؕ اِنَّ اللّٰهَ لَطِيْفٌ خَبِيْرٌ ﴿۱۷﴾

17. Ewe mwanangu! kwa hakika jambo lo lote lijapokuwa na uzito wa chembe ya hardali, likawa ndani ya mwamba au mbinguni au ardhini, Allah Atalileta; bila shaka Allah ni Latifu, Mwenye habari.

يٰبُنَىَّ اَقِمِ الصَّلٰوةَ وَاْمُرْ بِالْمَعْرُوْفِ وَانْهَ عَنِ الْمُنْكَرِ وَاصْبِرْ عَلٰى مَآ اَصَابَكَ ؕ اِنَّ ذٰلِكَ مِنْ عَزْمِ الْاُمُوْرِ ﴿۱۸﴾

18. Ewe mwanangu! simamisha Sala, na uamrishe mema, na kukataza mabaya, na usubiri juu ya yale yanayokusibu; hakika hayo ni miongoni mwa mambo muhimu sana.

Aya 15. *Wazazi wako.* Aya hii ni mojawapo katika zile zinazoagiza kuwatii wazazi. Kuwatii wazazi na kuwasaidia ni jambo la faradhi katika dini ya Kiislamu. Mtume s.a.w. alisema "Pepo iko chini ya miguu ya mama" (Kanzu-'Ummaal), yaani kumtii na kumtumikia kunaleta Pepo." Abu Hureira anasimulia ya kuwa mtu mmoja alimwuliza Mtume *s.a.w.*: Je nani anastahili zaidi nimfanyie ihsani? Mtume *s.a.w.* akajibu, Mama yako. Akauliza tena. Kisha nani? Mtume akajibu Mama yako. Akauliza tena kisha nani? Mtume akajibu mama yako. Akauliza tena kisha nani? Mtume *s.a.w.* akajibu Baba yako (Bukhari na Muslim). Tena anasimulia Abu Hureira: Mtume *s.a.w.* alisema, "Amedhalilika! Amedhalilika! Amedhalilika!!! Masahaba wakauliza, Nani Ee Mjumbe wa Allah? Akajibu, Mtu anayewaona baba yake au mama yake katika hali ya uzee kisha haingii Peponi."

Aya 16. *Basi usiwatii.* Hapa imeelezwa waziwazi kuwa kuwatii wazazi kuna kikomo. Wanapotaka mtoto wao amshirikishe Allah, au aache dini au kuvunja amri yo yote ya Allah, hapo asiwatii, ingawa ni juu ya mtoto kuendelea nao kwa urafiki mwema. Seyidna Ahmad, Masihi Aliyeahidiwa (*'alaihissalaam)*, amesema, "Mtu asiyewaheshimu wazazi wake, wala asiyezitii amri zao maarufu: zisizo kinyume cha Qur'an Takatifu, wala hawatumikii kwa haki, hayumo katika jamaa yangu" (Safina ya Nuhu).

وَلَا تُصَعِّرْ خَدَّكَ لِلنَّاسِ وَلَا تَمْشِ
فِي الْأَرْضِ مَرَحًا ۖ إِنَّ اللَّهَ لَا يُحِبُّ
كُلَّ مُخْتَالٍ فَخُورٍ ﴿١٩﴾
وَاقْصِدْ فِي مَشْيِكَ وَاغْضُضْ
مِنْ صَوْتِكَ ۚ إِنَّ أَنْكَرَ الْأَصْوَاتِ
لَصَوْتُ الْحَمِيرِ ﴿٢٠﴾ ع ٢

19. Wala usiwafanyie watu kiburi, wala usitembee katika nchi kwa maringo; hakika Allah Hampendi kila ajivunaye, ajifaharishaye.

20. Na ushike mwendo wa katikati, na uteremshe sauti yako; bila shaka sauti ya punda ni mbaya kuliko sauti zote.

FUNGU 3

أَلَمْ تَرَوْا أَنَّ اللَّهَ سَخَّرَ لَكُمْ مَا فِي
السَّمَاوَاتِ وَمَا فِي الْأَرْضِ وَأَسْبَغَ عَلَيْكُمْ
نِعَمَهُ ظَاهِرَةً وَبَاطِنَةً ۗ وَمِنَ النَّاسِ
مَنْ يُجَادِلُ فِي اللَّهِ بِغَيْرِ عِلْمٍ وَلَا هُدًى
وَلَا كِتَابٍ مُنِيرٍ ﴿٢١﴾
وَإِذَا قِيلَ لَهُمُ اتَّبِعُوا مَا أَنْزَلَ اللَّهُ قَالُوا بَلْ
نَتَّبِعُ مَا وَجَدْنَا عَلَيْهِ آبَاءَنَا ۗ أَوَلَوْ كَانَ
الشَّيْطَانُ يَدْعُوهُمْ إِلَىٰ عَذَابِ السَّعِيرِ ﴿٢٢﴾
وَمَنْ يُسْلِمْ وَجْهَهُ إِلَى اللَّهِ وَهُوَ مُحْسِنٌ
فَقَدِ اسْتَمْسَكَ بِالْعُرْوَةِ الْوُثْقَىٰ ۗ وَإِلَى اللَّهِ
عَاقِبَةُ الْأُمُورِ ﴿٢٣﴾

21. Je! hamwoni ya kwamba Allah Aliwatiishieni vilivyomo mbinguni na ardhini, na Akawakamilishieni neema Zake zilizo dhahiri na za siri? Na wako watu wanaobishana katika (mambo ya) Allah pasipo elimu wala mwongozo wala Kitabu chenye nuru.

22. Na wanapoambiwa, Fuateni Aliyoyateremsha Allah, husema: Bali tunafuata tuliyowakuta nayo baba zetu. Je, ijapokuwa Shetani anawaita kwenye adhabu ya Moto uwakao?

23. Na ajisalimishaye uso wake kwa Allah, naye ni mtenda mema, basi bila shaka amekwisha kamata kishikio kilicho madhubuti; na mwisho wa mambo yote ni kwa Allah.

Aya 20. Mauidha yote yaliyomo katika Aya hii na zilizotangulia ni mafunzo wanayopewa Waislamu wakifundishwa unyenyekevu. Na pia ni wazi kuwa Allah aliwapendelea watu wote kujua mwenendo mwema. Mambo ambayo Yesu alifundisha juu ya mlima ndiyo haya ambayo Lukmani aliyafundisha. Allah alizieneza neema Zake kila upande na mafundisho mema si kama alipewa Yesu na Waisraeli tu bali hata watu wa pande zingine za dunia.

Aya 23. *Ajisalimishaye,* yaani ajitupaye. Katika Aya hii mmeelezwa mambo mawili yaliyo sehemu mbili za dini ya Kiislamu: (1) kujisalimisha kwa Allah na kumwabudu yeye tu; na (2) kuwatendea wema viumbe.

وَمَنْ كَفَرَ فَلَا يَحْزُنْكَ كُفْرُهٗ ؕ اِلَيْنَا مَرْجِعُهُمْ فَنُنَبِّئُهُمْ بِمَا عَمِلُوْا ؕ اِنَّ اللّٰهَ عَلِيْمٌۢ بِذَاتِ الصُّدُوْرِ ﴿۲۴﴾

24. Na anayekufuru, basi isikuhuzunishe kufuru yake, marudio yao ni Kwetu, ndipo Tutawaambia yale waliyoyafanya; hakika Allah ni Mjuzi wa yaliyomo vifuani.

نُمَتِّعُهُمْ قَلِيْلًا ثُمَّ نَضْطَرُّهُمْ اِلٰى عَذَابٍ غَلِيْظٍ ﴿۲۵﴾

25. Tutawafaidisha kidogo, kisha Tutawaswaga kwenye adhabu ngumu.

وَلَئِنْ سَاَلْتَهُمْ مَّنْ خَلَقَ السَّمٰوٰتِ وَالْاَرْضَ لَيَقُوْلُنَّ اللّٰهُ ؕ قُلِ الْحَمْدُ لِلّٰهِ ؕ بَلْ اَكْثَرُهُمْ لَا يَعْلَمُوْنَ ﴿۲۶﴾

26. Na kama ukiwauliza, Ni nani aliyeziumba mbingu na ardhi? Bila shaka watasema: Allah. Sema: Sifa zote njema ni za Allah, lakini wengi wao hawajui.

لِلّٰهِ مَا فِي السَّمٰوٰتِ وَالْاَرْضِ ؕ اِنَّ اللّٰهَ هُوَ الْغَنِيُّ الْحَمِيْدُ ﴿۲۷﴾

27. Kila kilichomo mbinguni na ardhini ni cha Allah; hakika Allah ndiye Mkwasi, Mwenye kusifiwa.

وَلَوْ اَنَّ مَا فِي الْاَرْضِ مِنْ شَجَرَةٍ اَقْلَامٌ وَّالْبَحْرُ يَمُدُّهٗ مِنْۢ بَعْدِهٖ سَبْعَةُ اَبْحُرٍ مَّا نَفِدَتْ كَلِمٰتُ اللّٰهِ ؕ اِنَّ اللّٰهَ عَزِيْزٌ حَكِيْمٌ ﴿۲۸﴾

28. Na lau kama miti yote iliyomo ardhini ingalikuwa kalamu, na bahari Akaifanya wino, baada yake bahari nyingine saba, maneno ya Allah yasingalikwisha. Bila shaka Allah ni Mshindi Kamili, Mwenye hekima.

مَا خَلْقُكُمْ وَلَا بَعْثُكُمْ اِلَّا كَنَفْسٍ وَّاحِدَةٍ ؕ اِنَّ اللّٰهَ سَمِيْعٌۢ بَصِيْرٌ ﴿۲۹﴾

29. Si kuumbwa kwenu wala kufufuliwa kwenu ila kama nafsi moja tu; hakika Allah ni Asikiaye. Aonaye.

اَلَمْ تَرَ اَنَّ اللّٰهَ يُوْلِجُ الَّيْلَ فِي النَّهَارِ وَيُوْلِجُ النَّهَارَ فِي الَّيْلِ وَسَخَّرَ الشَّمْسَ وَالْقَمَرَ ۙ كُلٌّ يَّجْرِيْۤ اِلٰۤى اَجَلٍ مُّسَمًّى وَّاَنَّ اللّٰهَ بِمَا تَعْمَلُوْنَ خَبِيْرٌ ﴿۳۰﴾

30. Je, huoni ya kwamba Allah Huingiza usiku katika mchana, na Huingiza mchana katika usiku, na Amevitiisha jua na mwezi, vyote hupita mpaka wakati uliowekwa, na Allah Anazo habari za mnayoyatenda?

Aya 28. *Kalimaat*, "maneno." Wakristo kudhani Nabii Isa ni Mungu kwa sababu ameitwa "neno" hata katika Qur'an. Sasa hapa vitu vyote vya dunia vimetajwa ni "maneno" ya Allah. Je, wataviita navyo ni miungu? Kama vitu vingine vitakuwa si miungu japo vimeitwa "neno," pia Yesu hawezi kuwa Mungu kwa kuitwa "neno" katika Qur'an.

ذٰلِكَ بِاَنَّ اللّٰهَ هُوَ الْحَقُّ وَ اَنَّ مَا يَدْعُوْنَ
مِنْ دُوْنِهِ الْبَاطِلُ ۙ وَ اَنَّ اللّٰهَ هُوَ الْعَلِيُّ
الْكَبِيْرُ ﴿٣٠﴾ ع ٢

31. Hivi ni kwa sababu Allah ndiye Mkweli na wanachokiomba badala Yake ni batili, na bila shaka Allah Ndiye Mtukufu, Mkuu.

FUNGU 4

اَلَمْ تَرَ اَنَّ الْفُلْكَ تَجْرِيْ فِي الْبَحْرِ
بِنِعْمَتِ اللّٰهِ لِيُرِيَكُمْ مِّنْ اٰيٰتِهٖ ؕ اِنَّ
فِيْ ذٰلِكَ لَاٰيٰتٍ لِّكُلِّ صَبَّارٍ شَكُوْرٍ ﴿٣١﴾

32. Je, huoni kwamba merikebu hupita baharini kwa neema za Allah, ili Awaonyesheni Ishara Zake? Hakika katika hayo zimo Ishara kwa kila mwenye subira sana, mwenye shukrani.

وَ اِذَا غَشِيَهُمْ مَّوْجٌ كَالظُّلَلِ دَعَوُا اللّٰهَ
مُخْلِصِيْنَ لَهُ الدِّيْنَ ۚ فَلَمَّا نَجّٰىهُمْ اِلَى
الْبَرِّ فَمِنْهُمْ مُّقْتَصِدٌ ؕ وَمَا يَجْحَدُ بِاٰيٰتِنَآ
اِلَّا كُلُّ خَتَّارٍ كَفُوْرٍ ﴿٣٢﴾

33. Na wimbi linapowafunika kama vivuli, humwomba Allah kwa kumtii kweli kweli; lakini Anapowaokoa kuwaleta barani, baadhi yao hushika mwendo wa katikati, wala hapana azikanushaye Ishara Zetu ila kila mdanganyifu mkuu, kafiri mkubwa.

يٰۤاَيُّهَا النَّاسُ اتَّقُوْا رَبَّكُمْ وَاخْشَوْا يَوْمًا
لَّا يَجْزِيْ وَالِدٌ عَنْ وَّلَدِهٖ ۫ وَلَا مَوْلُوْدٌ
هُوَ جَازٍ عَنْ وَّالِدِهٖ شَيْـًٔا ؕ اِنَّ وَعْدَ اللّٰهِ حَقٌّ
فَلَا تَغُرَّنَّكُمُ الْحَيٰوةُ الدُّنْيَا ۪ وَلَا يَغُرَّنَّكُمْ
بِاللّٰهِ الْغَرُوْرُ ﴿٣٣﴾

34. Enyi watu, Mcheni Mola wenu na iogopeni siku ambayo haitamfaa baba kwa mtoto wake wala mtoto hatamfaa baba yake hata kidogo. Bila shaka ahadi ya Allah ni ya kweli, basi yasiwadanganyeni maisha ya dunia hii, wala asiwadanganyeni mdanganyi katika (mambo ya) Allah.

اِنَّ اللّٰهَ عِنْدَهٗ عِلْمُ السَّاعَةِ ۚ وَيُنَزِّلُ
الْغَيْثَ ۚ وَيَعْلَمُ مَا فِي الْاَرْحَامِ ؕ
وَمَا تَدْرِيْ نَفْسٌ مَّاذَا تَكْسِبُ غَدًا ؕ
وَمَا تَدْرِيْ نَفْسٌۢ بِاَيِّ اَرْضٍ تَمُوْتُ ؕ
اِنَّ اللّٰهَ عَلِيْمٌ خَبِيْرٌ ﴿٣٤﴾ ع ١٣

35. Kwa hakika elimu ya saa (ile) iko kwa Allah; naye Huteremsha mvua, na Huyajua yaliyomo matumboni; na nafsi yo yote haijui ni nini itakayoyachuma kesho, wala haijui nafsi itafia ardhi gani. Bila shaka Allah ni Mjuzi, Mwenye habari.

Aya 32. Aya hii inaashiria ya kuwa Waislamu ingawa pale walipewa udhia, walakini utafika wakati wataimiliki bahari.

سُوْرَةُ السَّجْدَةِ مَكِّيَّةٌ وَّ هِیَ مَعَ الْبَسْمَلَةِ اِحْدٰی وَ ثَلَا ثُوْنَ اٰیَةً وَّ ثَلَا ثَةُ رُکُوْعَاتٍ

32. SURA AS-SAJDA

Imeteremshwa Makka

Ina mafungu 3 na Aya 31 pamoja na Bismillahi

بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ ①

1. Kwa jina la Allah, Mwingi wa rehema, Mwingi wa ukarimu.

الٓمّٓ ②

2. Mimi ni Allah Nijuaye sana.

تَنْزِيْلُ الْكِتٰبِ لَا رَيْبَ فِيْهِ مِنْ رَّبِّ الْعٰلَمِيْنَ ③

3. Uteremsho wa Kitabu kisicho shaka ndani yake, umetoka kwa Mola wa walimwengu.

اَمْ يَقُوْلُوْنَ افْتَرٰىهُ ۚ بَلْ هُوَ الْحَقُّ مِنْ رَّبِّكَ لِتُنْذِرَ قَوْمًا مَّآ اَتٰىهُمْ مِّنْ نَّذِيْرٍ مِّنْ قَبْلِكَ لَعَلَّهُمْ يَهْتَدُوْنَ ④

4. Je, wanasema amekizua mwenyewe? Bali hicho ni haki itokayo kwa Mola wako ili uwaonye watu wasiofikiwa na Mwonyaji kabla yako, huenda wataongoka.

اَللّٰهُ الَّذِیْ خَلَقَ السَّمٰوٰتِ وَالْاَرْضَ وَمَا بَيْنَهُمَا فِیْ سِتَّةِ اَيَّامٍ ثُمَّ اسْتَوٰی عَلَی الْعَرْشِ ؕ مَا لَكُمْ مِّنْ دُوْنِهٖ مِنْ وَّلِیٍّ وَّلَا شَفِيْعٍ ؕ اَفَلَا تَتَذَكَّرُوْنَ ⑤

5. Allah ndiye Aliyeziumba mbingu na ardhi na vilivyomo kati yao katika nyakati sita, na Akastawi katika Arshi. Ninyi hamna mlinzi wala mwombezi isipokuwa Yeye tu, je, hamshiki nasaha?

يُدَبِّرُ الْاَمْرَ مِنَ السَّمَآءِ اِلَی الْاَرْضِ ثُمَّ يَعْرُجُ اِلَيْهِ فِیْ يَوْمٍ كَانَ مِقْدَارُهٗٓ اَلْفَ سَنَةٍ مِّمَّا تَعُدُّوْنَ ⑥

6. Hutengeneza jambo toka mbinguni mpaka ardhini; kisha linapanda Kwake katika siku ambayo kipimo chake ni miaka elfu mnayotumia katika kuhesabu.

Sura hii pia ilishuka Makka. Wanaosema kuwa baadhi ya Aya zake zilishuka Madina wanadhani tu.

Aya 2. Alif Laam Miim (Tazama sura 2:2).

Aya 3. *Laa raiba fiihi* "Kisicho shaka" pia maana yake ni "kisicho maangamizo." Mambo yote yaliyoelezwa katika Qur'an hayana dhara hata kidogo; na kama yafuatwe basi hayataleta ila heri tu (Pia tazama 2:3).

Aya 6. *Amr,* "jambo." Neno hili pia maana yake ni amri, hukumu, shauri, sheria na Qur'an.

ذٰلِكَ عٰلِمُ الْغَيْبِ وَالشَّهَادَةِ الْعَزِيْزُ الرَّحِيْمُ ۙ﴿۷﴾

7. Huyu ndiye Ajuaye mambo ya ghaibu na ya dhahiri, Mshindi kamili, Mrehemevu,

الَّذِيْٓ اَحْسَنَ كُلَّ شَيْءٍ خَلَقَهٗ وَبَدَاَ خَلْقَ الْاِنْسَانِ مِنْ طِيْنٍ ۚ﴿۸﴾

8. Ambaye Ameboresha umbo la kila kitu, na Akaanzisha umbo la mwanadamu kwa udongo.

ثُمَّ جَعَلَ نَسْلَهٗ مِنْ سُلٰلَةٍ مِّنْ مَّآءٍ مَّهِيْنٍ ۚ﴿۹﴾

9. Kisha Akafanya kizazi chake kwa mbegu ya maji yaliyo hafifu.

ثُمَّ سَوّٰىهُ وَنَفَخَ فِيْهِ مِنْ رُّوْحِهٖ وَجَعَلَ لَكُمُ السَّمْعَ وَالْاَبْصَارَ وَالْاَفْـِٕدَةَ ؕ قَلِيْلًا مَّا تَشْكُرُوْنَ ﴿۱۰﴾

10. Kisha Akamsawazisha na Akampulizia roho Yake. Na Akawapeni masikio na macho na mioyo. Lakini ni kidogo tu mnayoyashukuru.

وَقَالُوْٓا ءَاِذَا ضَلَلْنَا فِى الْاَرْضِ ءَاِنَّا لَفِىْ خَلْقٍ جَدِيْدٍ ؕ بَلْ هُمْ بِلِقَآئِ رَبِّهِمْ كٰفِرُوْنَ ﴿۱۱﴾

11. Nao husema: Je, tutakapotoweka ardhini, hakika tutarudishwa katika umbo jipya? Bali wao hawafikiri kwamba watakutana na Mola wao!

قُلْ يَتَوَفّٰىكُمْ مَّلَكُ الْمَوْتِ الَّذِىْ وُكِّلَ بِكُمْ ثُمَّ اِلٰى رَبِّكُمْ تُرْجَعُوْنَ ﴿۱۲﴾ ع ۱۴

12. Sema: Atawafisheni Malaika wa mauti aliyewakilishwa kwenu, kisha mtarejeshwa kwa Mola wenu.

FUNGU 2

وَلَوْ تَرٰٓى اِذِ الْمُجْرِمُوْنَ نَاكِسُوْا رُءُوْسِهِمْ عِنْدَ رَبِّهِمْ ؕ رَبَّنَآ اَبْصَرْنَا وَسَمِعْنَا فَارْجِعْنَا نَعْمَلْ صَالِحًا اِنَّا مُوْقِنُوْنَ ﴿۱۳﴾

13. Na ungaliwaona wakosefu wakiinamisha vichwa vyao mbele ya Mola wao, (na kusema:) Mola wetu! tumekwisha ona na tumekwisha sikia, basi Uturudishe tukafanye vitendo vizuri; hakika Sisi ni wenye yakini.

وَلَوْ شِئْنَا لَاٰتَيْنَا كُلَّ نَفْسٍ هُدٰىهَا وَلٰكِنْ حَقَّ الْقَوْلُ مِنِّىْ لَاَمْلَـَٔنَّ جَهَنَّمَ مِنَ الْجِنَّةِ وَالنَّاسِ اَجْمَعِيْنَ ﴿۱۴﴾

14. Na Tungalitaka, Tungempa kila mtu mwongozo wake, lakini imehakiki kauli iliyotoka Kwangu: Kwa yakini Nitaijaza Jahanamu kwa wote hawa majinni na watu.

Aya 10. Neno *fu'aad* kama linavyotumika katika Qur'an Tukufu halina maana ya moyo tu bali linaonyesha daraja la juu kabisa la uelewa. Tazama 28:11; 53:12; 46: 27 na 14:38.

Aya 14. *Imehakiki kauli iliyotoka Kwangu*, yaani amekwisha mpa kila mtu hiyari afuate anavyopenda, na hili hasa ndilo jambo bora maana linampandisha mwanandamu daraja za juu

فَذُوْقُوْا بِمَا نَسِيْتُمْ لِقَآءَ يَوْمِكُمْ هٰذَا ۚ
اِنَّا نَسِيْنٰكُمْ وَذُوْقُوْا عَذَابَ الْخُلْدِ بِمَا
كُنْتُمْ تَعْمَلُوْنَ ﴿١٥﴾

15. Basi ionjeni (adhabu) kwa sababu ya kusahau mkutano wa siku yenu hii; hakika Sisi Tumewasahauni, na onjeni adhabu idumuyo kwa sababu ya yale mliyokuwa mkiyatenda.

اِنَّمَا يُؤْمِنُ بِاٰيٰتِنَا الَّذِيْنَ اِذَا ذُكِّرُوْا بِهَا
خَرُّوْا سُجَّدًا وَّسَبَّحُوْا بِحَمْدِ رَبِّهِمْ وَهُمْ
لَا يَسْتَكْبِرُوْنَ ﴿١٦﴾ ۩

16. Hakika wanaoziamini Aya Zetu ni wale tu ambao wanapozikumbushwa huanguka kusujudu na kumtukuza Mola wao kwa (kutaja) sifa Zake, nao hawatakabari.

تَتَجَافٰى جُنُوْبُهُمْ عَنِ الْمَضَاجِعِ يَدْعُوْنَ
رَبَّهُمْ خَوْفًا وَّطَمَعًا ۖ وَّمِمَّا رَزَقْنٰهُمْ
يُنْفِقُوْنَ ﴿١٧﴾

17. Huinuka mbavu zao kutoka vitandani kumwomba Mola wao kwa hofu na tumaini, na hutoa katika yale Tuliyowapa.

فَلَا تَعْلَمُ نَفْسٌ مَّآ اُخْفِيَ لَهُمْ مِّنْ
قُرَّةِ اَعْيُنٍ ۚ جَزَآءًۢ بِمَا كَانُوْا يَعْمَلُوْنَ ﴿١٨﴾

18. Nafsi yo yote haijui walichofichiwa katika kinachofurahisha macho; ni malipo ya yale waliyokuwa wakiyafanya.

اَفَمَنْ كَانَ مُؤْمِنًا كَمَنْ كَانَ فَاسِقًا ۭ
لَا يَسْتَوٗنَ ﴿١٩﴾ وقف مقارن

19. Je! mumini anaweza kuwa sawa na yule aliye fasiki? Hawawi sawa.

اَمَّا الَّذِيْنَ اٰمَنُوْا وَعَمِلُوا الصّٰلِحٰتِ
فَلَهُمْ جَنّٰتُ الْمَاْوٰى ۭ نُزُلًۢا بِمَا كَانُوْا
يَعْمَلُوْنَ ﴿٢٠﴾

20. Ama wale walioamini na wakafanya vitendo vizuri; basi zitakuwa kwao Bustani za makao: makaribisho kwa yale waliyokuwa wakiyatenda.

وَاَمَّا الَّذِيْنَ فَسَقُوْا فَمَاْوٰىهُمُ النَّارُ ۭ
كُلَّمَآ اَرَادُوْٓا اَنْ يَّخْرُجُوْا مِنْهَآ اُعِيْدُوْا
فِيْهَا وَقِيْلَ لَهُمْ ذُوْقُوْا عَذَابَ النَّارِ الَّذِيْ
كُنْتُمْ بِهٖ تُكَذِّبُوْنَ ﴿٢١﴾

21. Lakini wale waliofanya uovu, basi kao lao ni Motoni; kila watakapotaka kutoka humo watarudishwa humo na wataambiwa: Onjeni adhabu ya Moto ambayo mlikuwa mkiikadhibisha.

---

kila wakati, kuliko kama angekuwa vivi hivi tu kama mashine asiyekosa wala asiyefanya wema, maana hapo hata asingestahili kupata zawadi yo yote.

Aya 18. Mtume *s.a.w.* anasema, Allah anasema, Nimewaandalia watumishi Wangu wema vitu ambavyo macho hayajapata kuviona, wala masikio hayajapata kuvisikia, wala havijapata kufikiriwa na moyo wa mtu (Bukhari).

Aya 19. *Fasiki.* Neno hili maana ni asi, avunjaye amri ya Allah, asiyekuballi haki, asherati, na ashikaye maovu.

وَلَنُذِيْقَنَّهُمْ مِّنَ الْعَذَابِ الْاَدْنٰى دُوْنَ
الْعَذَابِ الْاَكْبَرِ لَعَلَّهُمْ يَرْجِعُوْنَ ﴿٢٢﴾

22. Na kwa yakini Tutawaonjesha adhabu hafifu kabla ya adhabu kubwa huenda wakarejea (kwenye mwongozo).

وَمَنْ اَظْلَمُ مِمَّنْ ذُكِّرَ بِاٰيٰتِ رَبِّهٖ
ثُمَّ اَعْرَضَ عَنْهَا ؕ اِنَّا مِنَ الْمُجْرِمِيْنَ
مُنْتَقِمُوْنَ ﴿٢٣﴾ ع ١٥

23. Na ni nani mdhalimu mkubwa kuliko yule anayekumbushwa Aya za Mola wake kisha huzikengeuka? Hakika Sisi ni Wajilipizao kwa wakosefu.

FUNGU 3

وَلَقَدْ اٰتَيْنَا مُوْسَى الْكِتٰبَ فَلَا تَكُنْ
فِيْ مِرْيَةٍ مِّنْ لِّقَآئِهٖ وَجَعَلْنٰهُ هُدًى
لِّبَنِيْٓ اِسْرَآءِيْلَ ﴿٢٤﴾

24. Na bila shaka Tulimpa Musa Kitabu, basi usiwe na shaka ya kukutana Naye (Allah), na tukakifanya mwongozo kwa wana wa Israeli.

وَجَعَلْنَا مِنْهُمْ اَئِمَّةً يَّهْدُوْنَ بِاَمْرِنَا لَمَّا
صَبَرُوْا ؗ وَكَانُوْا بِاٰيٰتِنَا يُوْقِنُوْنَ ﴿٢٥﴾

25. Na Tukawafanya miongoni mwao maimamu wanaoongoza kwa amri Yetu waliposubiri; na walikuwa wakiziyakini Aya Zetu.

اِنَّ رَبَّكَ هُوَ يَفْصِلُ بَيْنَهُمْ يَوْمَ الْقِيٰمَةِ
فِيْمَا كَانُوْا فِيْهِ يَخْتَلِفُوْنَ ﴿٢٦﴾

26. Hakika Mola wako ndiye Atahukumu baina yao siku ya Kiyama katika yale waliyokuwa wakihitilafiana.

اَوَلَمْ يَهْدِ لَهُمْ كَمْ اَهْلَكْنَا مِنْ قَبْلِهِمْ
مِّنَ الْقُرُوْنِ يَمْشُوْنَ فِيْ مَسٰكِنِهِمْ ؕ اِنَّ
فِيْ ذٰلِكَ لَاٰيٰتٍ ؕ اَفَلَا يَسْمَعُوْنَ ﴿٢٧﴾

27. Je, hayawaongozi (kuona) ni vizazi vingapi Tuliviangamiza kabla yao vilivyokuwa vikitembea maskanini pao? Bila shaka katika hayo zimo Ishara; je, hawasikii?

Aya 22. *Laala watarejea.* Maneno haya yanaonyesha ya kwamba adhabu zinafika duniani ili kidogo kidogo ziwazuie watu katika maovu, wapate kuelekea kwa Allah.

Aya 24. *Min Liqaaihii,* "kwa kukutana nacho," yaani Kitabu kile kilichoahidiwa katika Kitabu cha Musa kwamba kitakuwa Sheria atakayopewa Mtume *s.a.w.* (Kumbukumbu 33:2).

Aya 25. Katika Aya hii zimeelezwa sifa nne za maimamu: (1). wanafanywa tu kuwa maimamu hali wao wenyewe hawakuwa na hamu ya jambo hilo wala hawakufanya mipango ya siri ili kufikia cheo hicho; (2) wanaongoza watu na mambo sawa na vile anavyoagiza Allah; (3) wanajizuia katika maovu, wanavumilia udhia wa makafiri na wanadumu katika hukumu za Mungu; (4) wanakuwa na yakini kamili juu ya Aya za Allah. Aya hii inaonyesha waziwazi kuwa maimamu wa namna hii wataendelea katika umati wa Mtume s.a.w. na haitakuwa taabu kuwatambua, kwani mifano yao imetokea mara nyingi katika mawalii na Manabii waliopita kabla yao.

اَوَلَمۡ يَرَوۡا اَنَّا نَسُوۡقُ الۡمَآءَ اِلَى الۡاَرۡضِ الۡجُرُزِ فَنُخۡرِجُ بِهٖ زَرۡعًا تَاۡكُلُ مِنۡهُ اَنۡعَامُهُمۡ وَاَنۡفُسُهُمۡ ؕ اَفَلَا يُبۡصِرُوۡنَ ﴿۲۸﴾ ع

28. Je, hawaoni ya kwamba Tunayaendesha maji kwenye ardhi kame kisha kwayo Tunaiotesha mimea wanayokula wanyama wao na wao wenyewe; je hawaoni?

وَيَقُوۡلُوۡنَ مَتٰى هٰذَا الۡفَتۡحُ اِنۡ كُنۡتُمۡ صٰدِقِيۡنَ ﴿۲۹﴾

29. Na wanasema: Ushindi huu utatokea lini ikiwa mnasema kweli?

قُلۡ يَوۡمَ الۡفَتۡحِ لَا يَنۡفَعُ الَّذِيۡنَ كَفَرُوۡۤا اِيۡمَانُهُمۡ وَلَا هُمۡ يُنۡظَرُوۡنَ ﴿۳۰﴾

30. Sema: Siku ya ushindi wale waliokufuru imani yao haitawafaa, wala hawatapewa muda wa kungoja.

فَاَعۡرِضۡ عَنۡهُمۡ وَانۡتَظِرۡ اِنَّهُمۡ مُّنۡتَظِرُوۡنَ ﴿۳۱﴾ ع ۱۶

31. Basi ujiepushe nao, na ngoja, hakika wao (pia) wanangoja.

سُوْرَةُ الْاَحْزَابِ مَدَنِيَّةٌ وَّ هِيَ مَعَ الْبَسْمَلَةِ اَرْبَعٌ وَّ سَبْعُوْنَ اٰيَةً وَّ تِسْعَةُ رُكُوْعَاتٍ

33. SURA AL-AHZAB

*I*meteremshwa Madina

Ina mafungu 9 na Aya 74 pamoja na Bismillahi

بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ ①

1. Kwa jina la Allah, Mwingi wa rehema, Mwingi wa ukarimu.

يٰۤاَيُّهَا النَّبِيُّ اتَّقِ اللّٰهَ وَلَا تُطِعِ الْكٰفِرِيْنَ وَالْمُنٰفِقِيْنَ ؕ اِنَّ اللّٰهَ كَانَ عَلِيْمًا حَكِيْمًا ۙ①

2. Ewe Nabii! Mche Allah wala usiwatii makafiri na wanafiki; bila shaka Allah ni Mjuzi, Mwenye hekima.

وَّاتَّبِعْ مَا يُوْحٰۤى اِلَيْكَ مِنْ رَّبِّكَ ؕ اِنَّ اللّٰهَ كَانَ بِمَا تَعْمَلُوْنَ خَبِيْرًا ۙ①

3. Na ufuate unayofunuliwa kutoka kwa Mola wako; kwa yakini Allah Anazo habari za mnayoyatenda.

وَّتَوَكَّلْ عَلَى اللّٰهِ ؕ وَكَفٰى بِاللّٰهِ وَكِيْلًا ①

4. Na utawakali kwa Allah; na Allah Atosha kuwa mlinzi.

مَا جَعَلَ اللّٰهُ لِرَجُلٍ مِّنْ قَلْبَيْنِ فِيْ جَوْفِهٖ ۚ وَمَا جَعَلَ اَزْوَاجَكُمُ الّٰٓـِٔيْ تُظٰهِرُوْنَ مِنْهُنَّ اُمَّهٰتِكُمْ ۚ وَمَا جَعَلَ اَدْعِيَآءَكُمْ

5. Allah Hakumwekea mwanadamu ye yote mioyo miwili kifuani mwake; wala Hakuwafanya wake zenu kuwa mama zenu kwa sababu tu ninyi mnawaita ni mama zenu

---

Sura hii imeitwa *Makundi* kwa kuhusiana na Makureishi waliounganika na makabila mengi ya Waarabu na Mayahudi na wakaenda Madina kwa vita kwenda kuwasaga kabisa Waislamu. Shambulio hilo kwa hakika lilikuwa kubwa mno walilopata kupelekewa Waislamu; na kushindwa kwa hawa maadui kulikuwa jambo la kustaajabisha mno lililopata kutokea duniani.

Sura hii ilishuka Madina, na tarehe yake inaweza kujulikana kwa kuona ya kuwa vita hivi vya waitifaki wa Makureishi vilitokea katika mwezi wa Shawwal (Mfunguo Mosi) katika mwaka wa nne wa Hijra (Bukhari). Habari zingine zilizoelezwa katika sura hii kama ndoa ya Mtume *s.a.w.* na bibi Zainab bint Jahsh zilitokea baadaye kidogo lakini si zaidi kuliko mwaka wa saba wa Hijra.

Aya 2. *Mungu ni Mjuzi, Mwenye hekima.* Katika sifa hizi imo dawa ya kumwepusha mtu na kufuru na unafiki. Kama mtu awe na yakini kuwa Mungu anajua habari zake zote, lazima atachelea maovu. Inasemekana ya kuwa Zuleikha aliponuia kumshawishi Nabii Yusuf kufanya naye maovu naye alilifunika sanamu lake alilokuwa akiliabudu. Alipoulizwa kwa nini analifunika alisema anaona haya, basi anataka lisimwone akifanya uovu ule. Basi kama mtu anaweza kuonea haya sanamu, siyo zaidi sana kwa Allah akiwa na yakini kuwa Mungu anajua kabisa habari zake? (Darsul Qur'an).

Aya 5. Aya hii imevunja desturi mbili zilizoshika sana katika mila za Waarabu. Desturi

اَبْنَآءَكُمْ ؕ ذٰلِكُمْ قَوْلُكُمْ بِاَفْوَاهِكُمْ ۚ
وَاللّٰهُ يَقُوْلُ الْحَقَّ وَهُوَ يَهْدِى السَّبِيْلَ ۝٤

wala Hakuwafanya watoto wenu wa kupanga kuwa wana wenu hasa. Hayo ni maneno tu ya vinywa vyenu ; Na Allah Husema kweli, Na ni Yeye Aongozae kwenye njia (iliyo sawa).

اُدْعُوْهُمْ لِاٰبَآئِهِمْ هُوَ اَقْسَطُ عِنْدَ اللّٰهِ ۚ
فَاِنْ لَّمْ تَعْلَمُوْٓا اٰبَآءَهُمْ فَاِخْوَانُكُمْ فِى
الدِّيْنِ وَمَوَالِيْكُمْ ؕ وَلَيْسَ عَلَيْكُمْ جُنَاحٌ
فِيْمَآ اَخْطَاْتُمْ بِهٖ ۙ وَلٰكِنْ مَّا تَعَمَّدَتْ
قُلُوْبُكُمْ ؕ وَكَانَ اللّٰهُ غَفُوْرًا رَّحِيْمًا ۝٥

6. Waiteni kwa (ubini wa) baba zao, maana huo ndiyo uadilifu mbele ya Allah. Na kama hamwajui baba zao, basi ni ndugu zenu katika dini na rafiki zenu. Wala si dhambi kwenu kwa yale mliyokosea, isipokuwa katika yale iliyoyafanya mioyo yenu kwa kusudi; na Allah ni Msamehevu, Mrehemevu.

اَلنَّبِىُّ اَوْلٰى بِالْمُؤْمِنِيْنَ مِنْ اَنْفُسِهِمْ ۚ
وَاَزْوَاجُهٗٓ اُمَّهٰتُهُمْ ؕ وَاُولُوا الْاَرْحَامِ
بَعْضُهُمْ اَوْلٰى بِبَعْضٍ فِىْ كِتٰبِ اللّٰهِ مِنَ
الْمُؤْمِنِيْنَ وَالْمُهٰجِرِيْنَ اِلَّآ اَنْ تَفْعَلُوْٓا
اِلٰٓى اَوْلِيٰٓئِكُمْ مَّعْرُوْفًا ؕ كَانَ ذٰلِكَ
فِى الْكِتٰبِ مَسْطُوْرًا ۝٦

7. Nabii ana haki zaidi kwa waaminio kuliko nafsi zao, na wakeze ni mama zao. Na wenye nasaba wana haki zaidi wao kwa wao katika Kitabu cha Allah kuliko waaminio na wahamiaji, lakini kama mkifanya wema kwa marafiki zenu si vibaya. Haya yamekwisha andikwa Kitabuni.

---

moja iliitwa *Dhihaar,* nayo ilikuwa namna ya kumwacha mke kwa muda naye asiweze kuolewa haidhuru kwa miaka mingapi akae hivyo. Ilikuwa ni kumwambia mke, "Wewe sasa kwangu u kama mgongo wa mama yangu." Jambo hili limekatazwa.

Desturi nyingine ilikuwa ya kupanga udugu. Wanaopangana udugu au ubaba na utoto wanakuwa kama ndugu kweli katika mambo yote. Basi desturi hii imekatazwa na inasemwa haiwezekani ujamaa au udugu au utoto wa kupanga uwe sawa na udugu wa damu.

Aya 7. *Wakeze ni mama zao.* Wake wa Manabii wa Allah wanakuwa mama za wafuasi wao kwa sababu ya heshima.

Wenye nasaba wana haki zaidi, yaani haki ya kurithiana. Udugu wa dini hauingii kwenye kurithiana isipokuwa mwenye mali awe alifanya wasia wa kumpa zawadi, na hata hivyo zawadi hiyo haitakubaliwa kuzidi thuluthi moja ya mali.

وَاِذْ اَخَذْنَا مِنَ النَّبِيّٖنَ مِيْثَاقَهُمْ وَمِنْكَ
وَمِنْ نُّوْحٍ وَّاِبْرٰهِيْمَ وَمُوْسٰى وَعِيْسَى
ابْنِ مَرْيَمَ ۠ وَاَخَذْنَا مِنْهُمْ مِّيْثَاقًا غَلِيْظًا ۙ﴿۷﴾

8. Na Tulipoahidiana na Manabii na wewe, na Nuhu na Ibrahimu, na Musa na Isa mwana wa Mariamu na Tuliahidiana nao ahadi ngumu,

لِّيَسْـَٔلَ الصّٰدِقِيْنَ عَنْ صِدْقِهِمْ ۚ وَاَعَدَّ
لِلْكٰفِرِيْنَ عَذَابًا اَلِيْمًا ﴿۸﴾ ع ۱۷

9. Ili Awaulize wakweli juu ya ukweli wao, na Amewaandalia makafiri adhabu iumizayo.

FUNGU 2

يٰٓاَيُّهَا الَّذِيْنَ اٰمَنُوا اذْكُرُوْا نِعْمَةَ اللّٰهِ
عَلَيْكُمْ اِذْ جَآءَتْكُمْ جُنُوْدٌ فَاَرْسَلْنَا
عَلَيْهِمْ رِيْحًا وَّجُنُوْدًا لَّمْ تَرَوْهَا ؕ وَكَانَ
اللّٰهُ بِمَا تَعْمَلُوْنَ بَصِيْرًا ۚ﴿۹﴾

10. Enyi mlioamini! kumbukeni neema za Allah zilizo juu yenu yalipowafikieni majeshi, basi Tukawapelekea upepo na majeshi msiyoyaona, na Allah Anayaona mnayoyafanya.

اِذْ جَآءُوْكُمْ مِّنْ فَوْقِكُمْ وَمِنْ اَسْفَلَ
مِنْكُمْ وَاِذْ زَاغَتِ الْاَبْصَارُ وَبَلَغَتِ
الْقُلُوْبُ الْحَنَاجِرَ وَتَظُنُّوْنَ بِاللّٰهِ الظُّنُوْنَا ﴿۱۰﴾

11. Walipowajieni (kuwasha-mbulieni) kutoka juu yenu na kutoka chini yenu; na macho yaliponywea na mioyo ikapanda kooni, nanyi mkaanza kumdhania Allah dhana mbalimbali.

هُنَالِكَ ابْتُلِيَ الْمُؤْمِنُوْنَ وَزُلْزِلُوْا زِلْزَالًا
شَدِيْدًا ﴿۱۱﴾

12. Hapo waaminio walijaribiwa na wakatetemeshwa kwa tetemesho kali.

Aya 8. Ahadi iliyotajwa hapa inasemekana ni ahadi ya kufikisha ujumbe wa Mungu sawasawa Baidhawi).

Aya 10. Toka Aya hii zimeanza habari za vita vya *Ahzaab* au pia vinaitwa vya Handaki. Vimeitwa vya *Ahzaab* (makundi) kwa sababu ya makundi ya makabila tisa mbalimbali ya Waarabu na Mayahudi yapatayo watu elfu kumi waliojumuika wote kwa umoja ili kuwasaga Waislamu. Vimeitwa vya handaki kwa sababuWaislamu Madina walichimba handaki kuuzunguka mji ambalo liliwazuia makafiri wasiweze kuivamia Madina kiholela. Kabila moja katika Mayahudi, Banu Kuraidha, lilikuwa katika mkataba wa kusaidiana na Waislamu ikitokea vita, lakini wakati huu likapinduka na kujiunga pamoja na maadui wa Waislamu. Vita hii iliendelea kwa siku saba. Siku ya saba makafiri wakafikiwa na dhoruba kali ya upepo ambayo Sir William Muir anaieleza hivi: Katika hali ya kuchoka na nyoyo zimeingia baridi, ukawaingilia usiku wenye baridi na tufani. Upepo na mvua vikaipiga kambi yao isiyohifadhiwa vibaya-vibaya. Tufani ikazidi ikawa kimbunga. Mioto yao ikazimika, mahema yao yakang'olewa, vyombo vya kupikia na vitu vingine vikasambazwa." Basi hivi ndivyo Allah alivyowasaidia waaminio, na makafiri wakalazimika kukimbia.

وَاِذْ يَقُوْلُ الْمُنٰفِقُوْنَ وَالَّذِيْنَ فِيْ قُلُوْبِهِمْ مَّرَضٌ مَّا وَعَدَنَا اللّٰهُ وَرَسُوْلُهٗٓ اِلَّا غُرُوْرًا ﴿١٢﴾

13. Na waliposema wanafiki na wale wenye maradhi mioyoni mwao, Allah na Mtume wake hawakutuahidi ila udanganyifu tu.

وَاِذْ قَالَتْ طَّآئِفَةٌ مِّنْهُمْ يٰٓاَهْلَ يَثْرِبَ لَا مُقَامَ لَكُمْ فَارْجِعُوْا ۚ وَيَسْتَاْذِنُ فَرِيْقٌ مِّنْهُمُ النَّبِيَّ يَقُوْلُوْنَ اِنَّ بُيُوْتَنَا عَوْرَةٌ ۛ وَمَا هِيَ بِعَوْرَةٍ ۛ اِنْ يُّرِيْدُوْنَ اِلَّا فِرَارًا ﴿١٣﴾

14. Na taifa moja miongoni mwao liliposema: Enyi wenyeji wa Yathrib! Hapa si mahali pa kukaa ninyi basi rudini; na kundi jingine miongoni mwao likaomba ruhusa kwa Mtume kwa kusema: Hakika nyumba zetu hazina ulinzi, lakini hazikuwa bila ulinzi, hawakutaka ila kukimbia tu.

وَلَوْ دُخِلَتْ عَلَيْهِمْ مِّنْ اَقْطَارِهَا ثُمَّ سُئِلُوا الْفِتْنَةَ لَاٰتَوْهَا وَمَا تَلَبَّثُوْا بِهَآ اِلَّا يَسِيْرًا ﴿١٤﴾

15. Na lau kama yangaliingizwa (majeshi) juu yao katika pande zote (za Madina), kisha wakaombwa kufanya vita (juu ya Waislamu) wangeifanya, na wasingelikaa humo ila muda kidogo tu.

وَلَقَدْ كَانُوْا عَاهَدُوا اللّٰهَ مِنْ قَبْلُ لَا يُوَلُّوْنَ الْاَدْبَارَ ۭ وَكَانَ عَهْدُ اللّٰهِ مَسْـُٔوْلًا ﴿١٥﴾

16. Na kwa yakini walikwisha muahidi Allah hapo kabla ya kwamba hawatageuza migongo (hawatakimbia); na ahadi ya Allah ni yenye kuulizwa.

قُلْ لَّنْ يَّنْفَعَكُمُ الْفِرَارُ اِنْ فَرَرْتُمْ مِّنَ الْمَوْتِ اَوِ الْقَتْلِ وَاِذًا لَّا تُمَتَّعُوْنَ اِلَّا قَلِيْلًا ﴿١٦﴾

17. Sema: Kukimbia hakutawafaeni asilan, kama mkiyakimbia mauti au kupigana; na ndipo hamtanufaishwa ila kidogo.

قُلْ مَنْ ذَا الَّذِيْ يَعْصِمُكُمْ مِّنَ اللّٰهِ اِنْ اَرَادَ بِكُمْ سُوْۗءًا اَوْ اَرَادَ بِكُمْ رَحْمَةً ۭ وَلَا يَجِدُوْنَ لَهُمْ مِّنْ دُوْنِ اللّٰهِ وَلِيًّا وَّلَا نَصِيْرًا ﴿١٧﴾

18. Sema: Ni nani ambaye aweza kuwalindeni na Allah kama Yeye Awatakieni dhara, au kuwatakieni rehema? Wala hawatapata mlinzi wala msaidizi kinyume cha Allah.

قَدْ يَعْلَمُ اللّٰهُ الْمُعَوِّقِيْنَ مِنْكُمْ وَالْقَاۗىِٕلِيْنَ لِاِخْوَانِهِمْ هَلُمَّ اِلَيْنَا ۚ وَلَا يَاْتُوْنَ الْبَاْسَ اِلَّا قَلِيْلًا ﴿١٨﴾

19. Bila shaka Allah Anawajua wale wanaojizuia miongoni mwenu na wawaambiao ndugu zao: Njooni kwetu: wala hawafiki kwenye mapigano ila kidogo,

Aya 14. *Yathrib.* Mji wa Madina kabla ya kufika kwa Mtume *s.a.w.* ulikuwa ukiitwa Yathrib.

20. Wakiwafanyieni choyo; lakini inapofika hofu, utawaona wanakutazama, macho yao yanazunguka-zunguka kama yule aliyezimia kwa mauti; lakini hofu inapoondoka, wanawaudhini kwa ndimi kali, wakifanya choyo juu ya heri. Hao hawakuamini, kwa hiyo Allah Ameviharibu vitendo vyao, na hayo ni rahisi kwa Allah.

اَشِحَّةً عَلَيْكُمْ ۚ فَاِذَا جَآءَ الْخَوْفُ
رَاَيْتَهُمْ يَنْظُرُوْنَ اِلَيْكَ تَدُوْرُ اَعْيُنُهُمْ
كَالَّذِيْ يُغْشٰى عَلَيْهِ مِنَ الْمَوْتِ ۚ فَاِذَا
ذَهَبَ الْخَوْفُ سَلَقُوْكُمْ بِاَلْسِنَةٍ حِدَادٍ
اَشِحَّةً عَلَى الْخَيْرِ ؕ اُولٰٓئِكَ لَمْ يُؤْمِنُوْا
فَاَحْبَطَ اللّٰهُ اَعْمَالَهُمْ ؕ وَكَانَ ذٰلِكَ
عَلَى اللّٰهِ يَسِيْرًا ۝٢٠

21. Wanafikiri makundi haya haya-jaondoka. Na kama makundi yangekuja (tena), wangependa laiti wangekaa jangwani kwa Mabedui wakiuliza habari zenu. Na kama wangalikuwa pamoja nanyi wasingalipigana ila kidogo tu.

يَحْسَبُوْنَ الْاَحْزَابَ لَمْ يَذْهَبُوْا ۚ وَاِنْ
يَّاْتِ الْاَحْزَابُ يَوَدُّوْا لَوْ اَنَّهُمْ بَادُوْنَ
فِي الْاَعْرَابِ يَسْاَلُوْنَ عَنْ اَنْۢبَآئِكُمْ ؕ
وَلَوْ كَانُوْا فِيْكُمْ مَّا قٰتَلُوْٓا اِلَّا قَلِيْلًا ۝٢٠ ع ٣

FUNGU 3

22. Bila shaka mnao mfano mwema kwa Mtume wa Allah, kwa mwenye kumwogopa Allah na siku ya Mwisho, na kumtaja sana Allah.

لَقَدْ كَانَ لَكُمْ فِيْ رَسُوْلِ اللّٰهِ اُسْوَةٌ
حَسَنَةٌ لِّمَنْ كَانَ يَرْجُوا اللّٰهَ وَالْيَوْمَ الْاٰخِرَ
وَذَكَرَ اللّٰهَ كَثِيْرًا ۝٢١

23. Na waaminio walipoyaona majeshi, walisema: Haya ndiyo Aliyotuahidi Allah na Mtume Wake, na Allah na Mtume Wake wamesema kweli; na haikuwazidishia ila imani na utii.

وَلَمَّا رَاَ الْمُؤْمِنُوْنَ الْاَحْزَابَ ۙ قَالُوْا
هٰذَا مَا وَعَدَنَا اللّٰهُ وَرَسُوْلُهٗ وَصَدَقَ
اللّٰهُ وَرَسُوْلُهٗ ۫ وَمَا زَادَهُمْ اِلَّاۤ اِيْمَانًا
وَّتَسْلِيْمًا ۝٢٢

Aya 22. *Mnao mfano mwema katika Mtume wa Allah.* Mtume Muhammad *s.a.w.* kila jambo alilofundisha lilimpitia katika maisha yake: alikuwa yatima, akawa kijana mwenye kufanya kazi. Alikuwa maskini, alipata kuwatumikisha watu, alikuwa tajiri, alioa, alizaa, alifiwa, alikuwa askari na jemadari, alikuwa mtawala na mfalme na kiongozi. Ilmuradi alipitia maisha yote ya kibinadamu na hivyo akaweka mfano mwema kwa ajili ya watu wa kila namna. Na ukitazama mafundisho yake, hakuna hata jambo dogo lililopungua, kila kitu hata namna ya kula, kulala, kutembea na kadha wa kadha, kimefundishwa. Kwa neno zima sifa hizi ni maalum kwa ajili ya Mtume Muhammad tu. Yesu kwa mfano, hakuoa, hakuzaa, hakutawala, hakufanyia watu kazi, hakuwa askari, hakufiwa n.k.w. basi angewezaje kuonyesha mfano juu ya mambo hayo muhimu yanayowapitia watu kila siku?

Aya 23. Waaminio walipoona majeshi yale hawakutapatapa kama wanafiki, bali walijua ya kuwa ahadi iliyotolewa katika sura 38:12 sasa itatimia, na tukio hili likawazidishia imani.

مِنَ الْمُؤْمِنِيْنَ رِجَالٌ صَدَقُوْا مَا عَاهَدُوا
اللّٰهَ عَلَيْهِ ۚ فَمِنْهُمْ مَّنْ قَضٰى نَحْبَهٗ
وَمِنْهُمْ مَّنْ يَّنْتَظِرُ ۖ وَمَا بَدَّلُوْا
تَبْدِيْلًا ﴿٢٣﴾

24. Wapo watu miongoni mwa waaminio waliotimiza ahadi waliyoahidiana na Allah: hivyo baadhi yao wamekwisha maliza nadhiri zao, na wako miongoni mwao wanaongojea, wala hawakubadilika hata kidogo.

لِّيَجْزِيَ اللّٰهُ الصّٰدِقِيْنَ بِصِدْقِهِمْ وَيُعَذِّبَ
الْمُنٰفِقِيْنَ اِنْ شَآءَ اَوْ يَتُوْبَ عَلَيْهِمْ ۭ اِنَّ
اللّٰهَ كَانَ غَفُوْرًا رَّحِيْمًا ﴿٢٤﴾

25. Ili Allah Awalipe wakweli kwa sababu ya ukweli wao, na kuwaadhibu wanafiki kama Akipenda, au kuwageukia (kwa rehema). Bila shaka Allah ni Msamehevu, Mrehemevu.

وَرَدَّ اللّٰهُ الَّذِيْنَ كَفَرُوْا بِغَيْظِهِمْ لَمْ يَنَالُوْا
خَيْرًا ۭ وَكَفَى اللّٰهُ الْمُؤْمِنِيْنَ الْقِتَالَ ۭ
وَكَانَ اللّٰهُ قَوِيًّا عَزِيْزًا ﴿٢٥﴾

26. Na waliomkufuru Allah Amewarudisha na ghadhabu yao; hawakupata cho chote katika heri; na Allah Amewatoshea waaminio katika mapigano. Na Allah ni Mwenye uwezo, Mwenye ushindi kamili.

وَاَنْزَلَ الَّذِيْنَ ظَاهَرُوْهُمْ مِّنْ
اَهْلِ الْكِتٰبِ مِنْ صَيَاصِيْهِمْ وَقَذَفَ
فِيْ قُلُوْبِهِمُ الرُّعْبَ فَرِيْقًا تَقْتُلُوْنَ
وَتَاْسِرُوْنَ فَرِيْقًا ﴿٢٦﴾

27. Na Akawateremsha wale waliowasaidia (maadui) katika watu wa Kitabu kutoka katika ngome zao, na Akatia hofu katika mioyo yao: baadhi yao mnawaua na wengine mnawateka.

Aya 24. Waliomaliza nadhiri zao ni wale waliokwisha uawa katika njia ya Allah na wakafa mashahidi; na wanaongojea ni wale waaminio walio bado hai wenye shauku ya kuilinda njia ya Allah hata kwa uhai wao.

Aya 27. *Baadhi mnawauwa,* yaani Mayahudi wa kabila la Banu Kuraidha tuliokwisha wataja. Mayahudi hawa walivunja mapatano ya kusaidiana na Waislamu na wakasaidia maadui wa Waislamu kwa upande wa ndani wa Madina ili Waislamu washindwe na wauawe upesi.

Yale majeshi ya maadui yalipokimbia, hawa Banu Kuraidha pia wakaenda jifungia ndani ya ngome zao. Mtume s.a.w. ikawa lazima aende kuwauliza kwa nini wamevunja uaminifu, isije akakaa na watu ambao ni maadui wanaoweza kuleta matata baadaye, bila kuziba chokochoko zao.

Kwanza akamtuma Seyidna Ali aende akawaulize kwa nini walivunja mapatano. Banu Kuraidha wasijali. Wakaanza kumtukana Seyidna Ali pamoja na wenzake aliotumwa nao, wakamtukana Mtume s.a.w. na wakeze na binti yake kwa matusi machafu kabisa.

Basi Mtume pamoja na jeshi wakaihusuru ngome yao. Mayahudi wakaanza kupigana. Lakini wakaona hawawezi kuendelea, wakaangukia, ila wasikubali Mtume kuwakatia hukumu ambayo ingekuwa ya kuwafukuza watoke Madina kama walivyofukuzwa wenzao zamani. Baadhi ya

28. Na Akawarithisheni ardhi yao na majumba yao na mali zao, na ardhi msiyoikanyaga. Na Allah ni Mwenye uwezo juu ya kila kitu.

وَ اَوْرَثَكُمْ اَرْضَهُمْ وَ دِيَارَهُمْ
وَ اَمْوَالَهُمْ وَ اَرْضًا لَّمْ تَطَـُٔوْهَا ؕ
وَ كَانَ اللّٰهُ عَلٰى كُلِّ شَىْءٍ قَدِيْرًا ﴿۲۷﴾ ع ۱۹

FUNGU 4

29. Ewe Nabii! waambie wake zako: Ikiwa mnapenda maisha ya dunia hii na uzuri wake, haya njooni, nitawapeni matumizi na nitawasindikizeni kwa msindikizo mzuri.

يٰۤاَيُّهَا النَّبِىُّ قُلْ لِّاَزْوَاجِكَ اِنْ كُنْتُنَّ
تُرِدْنَ الْحَيٰوةَ الدُّنْيَا وَ زِيْنَتَهَا فَتَعَالَيْنَ
اُمَتِّعْكُنَّ وَ اُسَرِّحْكُنَّ سَرَاحًا جَمِيْلًا ﴿۲۸﴾

Mayahudi wakaanza kuwalaumu wenzao kuwa wamefanya hiyana mbaya, na kuwa Islam ni haki na afadhali waingie Uislamu. Lakini wengi wao wasikubali shauri hili.

Mwishoni wakataka shauri lao likatwe na Sa'ad bin Mu'aadh (Bukhari, Tabari, na Khamis). Mtume *s.a.w* akakubali hili ombi lao. Huyu Sa'ad alikuwa mkubwa wa kabila la Aus. Na hawa Aus walikuwa rafiki za Banu Kuraidha. Ndiyo maana wakataka wahukumiwe naye. Watu wa kabila la Aus wakamzunguka Sa'ad wakimwomba awahurumie rafiki zao Banu Kuraidha. Wakaenda naye wamemzunguka mpaka penye ngome. Sa'ad akawauliza Mayahudi: Je mtakubali hukumu yangu? Wakajibu, Ndiyo. Akaonyesha hali anaona haya upande aliokaa Mtume *s.a.w.* akawauliza, Je, mtakubali hukumu yangu? Mtume *s.a.w.* akajibu, Ndiyo. Akawaelekea watu wa kabila la Aus akawauliza, je, mtakubali hukumu yangu? nao wakajibu, Ndiyo. (Tabari na Hisham). Basi Sa'ad akatoa hukumu yake sawa na amri hii ya Biblia ambacho ni Kitabu cha dini ya Mayahudi, isemayo hivi:

> "Unapoukaribia mji kupigana nao, unadie amani. Na itakuwa, ukikupa jibu la amani, na kuwafungulieni, basi itakuwa ya kwamba watu wote waliomo humo watakuwa mateka kwenu na watawatumikieni. Na kama hautafanya amani nanyi, bali utafanya vita nanyi, nanyi mtauhusuru: Na Bwana Mungu wako atakapoutoa mikononi mwako, wewe utampiga kila mwanamume wa humo kwa ncha ya upanga: Lakini wanawake na watoto, na wanyama, na vyote vilivyomo katika mji hata mateka wewe utachukua." (Kumbukumbu 20:10-18).

Kwa mafundisho haya ya Kiyahudi, kama wao wangewashinda Waislamu wanaume wote wangeuawa, na watoto na wanawake wote wangetiwa utumwani. Basi Bwana Sa'ad alitoa hukumu kuwa Mayahudi wauawe sawa na amri ya dini yao. Kama wangekubali waamuliwe na Mtume wangepata adhabu nyepesi: lakini sasa ilikuwa haiwezekani kwa vile pande zote zilikwisha kubali kuwa zitatii amri ya Sa'ad ambaye wao wenyewe ndio waliomchagua kuwa hakimu. Na kwa njia hii kudra ya Allah ikamalizika.

Aya 28. *Nchi msiyoikanyaga.* Hapa Waislamu wanaahidiwa watarithishwa pia nchi zingine wasizozikanyaga, na baadaye nchi hizo zikaingia katika mamlaka ya Waislamu.

Aya 29. Waislamu walipowashinda Banu Kuraidha mali nyingi iliingia mikononi mwao. Mtume *s.a.w.* aliwagawanyia Waislamu wengine lakini wakeze asiwape. Wakeze wakaona mbona wao wasipate hali sasa umekuwa wakati wa neema. Wakamfikia Mtume kwa pamoja wakampa shauri lao kwamba nao wapate. Mtume hakupenda wajiingize ndani ya tamaa ya vitu vya dunia. Basi alijitenga nao, kwa mwezi mzima asiwafikie. Basi Allah akateremsha Aya hii.

وَاِنْ كُنْتُنَّ تُرِدْنَ اللّٰهَ وَرَسُوْلَهٗ وَالدَّارَ الْاٰخِرَةَ فَاِنَّ اللّٰهَ اَعَدَّ لِلْمُحْسِنٰتِ مِنْكُنَّ اَجْرًا عَظِيْمًا ﴿٢٩﴾

30. Na kama mnamtaka Allah na Mtume Wake na nyumba ya Akhera, basi kwa hakika Allah Amewaandalia wafanyao mema miongoni mwenu malipo makubwa.

يٰنِسَآءَ النَّبِيِّ مَنْ يَّاْتِ مِنْكُنَّ بِفَاحِشَةٍ مُّبَيِّنَةٍ يُّضٰعَفْ لَهَا الْعَذَابُ ضِعْفَيْنِ ؕ وَكَانَ ذٰلِكَ عَلَى اللّٰهِ يَسِيْرًا ﴿٣٠﴾

31. Enyi wake wa Nabii! atakayefanya ubaya dhahiri miongoni mwenu, atazidishiwa adhabu mara mbili; na haya ni rahisi kwa Allah.

JUZU 22

وَمَنْ يَّقْنُتْ مِنْكُنَّ لِلّٰهِ وَرَسُوْلِهٖ وَتَعْمَلْ صَالِحًا نُّؤْتِهَآ اَجْرَهَا مَرَّتَيْنِ ۙ وَاَعْتَدْنَا لَهَا رِزْقًا كَرِيْمًا ﴿٣١﴾

32. Na miongoni mwenu atakayemtii Allah na Mtume Wake, na kutenda mema, Tutampa malipo yake mara mbili, na kumwandalia riziki yenye heshima.

يٰنِسَآءَ النَّبِيِّ لَسْتُنَّ كَاَحَدٍ مِّنَ النِّسَآءِ اِنِ اتَّقَيْتُنَّ فَلَا تَخْضَعْنَ بِالْقَوْلِ فَيَطْمَعَ الَّذِيْ فِيْ قَلْبِهٖ مَرَضٌ وَّقُلْنَ قَوْلًا مَّعْرُوْفًا ﴿٣٢﴾

33. Enyi wake wa Nabii, ninyi si kama ye yote katika wanawake kama mkimcha (Mungu), basi msiwe laini katika usemi ili asitamani mtu mwenye ugonjwa moyoni mwake, na semeni kauli njema.

Mtume *s.a.w.* kwanza akamwuliza Aisha. Aisha akajibu kuwa anamtaka Allah na Mtume Wake, hataki vitu vya dunia. Aliwauliza wakeze wote mbalimbali, na wote wakajibu kama alivyojibu Aisha (Bukhari). Basi akakaa nao. Kama Mtume s.a.w. angekuwa ni mtu tu kama watu wa kidunia, bila shaka angeanza kujaza nyumbani kwake; lakini Mtume hakujali vitu vya dunia, na aliona fahari katika umaskini; hata alikuwa anasema, "Ufakiri ni fahari yangu."

Tukio hili linaonyesha waziwazi kuwa Mtume *s.a.w.* hakuoa wakeze kwa kutaka anasa, kama wanavyomlaumu Wakristo, maana angewaoa kwa sababu hii asingechukua wanawake wazee-wazee kama walivyokuwa wakeze wengi. Zaidi ya hayo angeangalia sana kuwapendeza na kuwaridhisha, wala asingekuwa tayari kuwaacha kwa kuwa wametaka vitu ambavyo alikuwa na uwezo kamili wa kuwapa.

Aya 32. *Tutampa malipo yake mara mbili,* ndiyo kusema atapewa malipo mengi, maana amejizuia katika maisha ya raha duniani, basi lazima malipo yake yawe zaidi katika Akhera.

Aya 33. Ingawa amri hii imeagizwa kwa wake wa Mtume *s.a.w.* lakini inawahusu wanawake wote wa Kiislamu.

وَقَرْنَ فِيْ بُيُوْتِكُنَّ وَلَا تَبَرَّجْنَ تَبَرُّجَ الْجَاهِلِيَّةِ الْاُوْلٰى وَاَقِمْنَ الصَّلٰوةَ وَاٰتِيْنَ الزَّكٰوةَ وَاَطِعْنَ اللّٰهَ وَرَسُوْلَهٗ ؕ اِنَّمَا يُرِيْدُ اللّٰهُ لِيُذْهِبَ عَنْكُمُ الرِّجْسَ اَهْلَ الْبَيْتِ وَيُطَهِّرَكُمْ تَطْهِيْرًا ﴿۳۴﴾

34. Na kaeni majumbani mwenu, wala msionyeshe mapambo sawa na maonesho ya ujinga wa zamani; na simamisheni Sala, na toeni Zaka, na Mtiini Allah na Mtume Wake. Allah Anataka tu kuwaondoleeni uchafu, enyi watu wa nyumbani, na kuwatakaseni kabisa.

وَاذْكُرْنَ مَا يُتْلٰى فِيْ بُيُوْتِكُنَّ مِنْ اٰيٰتِ اللّٰهِ وَالْحِكْمَةِ ؕ اِنَّ اللّٰهَ كَانَ لَطِيْفًا خَبِيْرًا ﴿۳۵﴾ ع

35. Na kumbukeni yasomwayo majumbani mwenu katika Aya za Allah na hekima; kwa hakika Allah ni Mpole, Mwenye habari.

FUNGU 5

اِنَّ الْمُسْلِمِيْنَ وَالْمُسْلِمٰتِ وَالْمُؤْمِنِيْنَ وَالْمُؤْمِنٰتِ وَالْقٰنِتِيْنَ وَالْقٰنِتٰتِ وَالصّٰدِقِيْنَ وَالصّٰدِقٰتِ وَالصّٰبِرِيْنَ وَالصّٰبِرٰتِ وَالْخٰشِعِيْنَ وَالْخٰشِعٰتِ وَالْمُتَصَدِّقِيْنَ وَالْمُتَصَدِّقٰتِ وَالصَّآئِمِيْنَ وَالصّٰٓئِمٰتِ وَالْحٰفِظِيْنَ فُرُوْجَهُمْ وَالْحٰفِظٰتِ وَالذّٰكِرِيْنَ اللّٰهَ كَثِيْرًا

36. Bila shaka wanaume wanaojisalimisha na wanawake wanaojisalimisha, na wanaume wanaoamini na wanawake wanaoamini, na wanaume wanaotii na wanawake wanaotii, na wanaume wasemao kweli na wanawake wasemao kweli, na wanaume wanaosubiri na wanawake wanaosubiri, na wanaume wanaonyenyekea na wanawake wanaonyenyekea, na wanaume wanaotoa sadaka na wanawake wanaotoa sadaka, na wanaume wanaofunga saumu na wanawake wanaofunga saumu, na wanaume wanaolinda tupu zao na

Aya 34. *Anataka tu kuwaondoleeni.* Mkewe Mtume, Maria Kibtiya alikuwa Mkristo; Safiya alikuwa Myahudi; basi waliondolewa uchafu wa itikadi mbaya na mila zisizofaa, na namna hii wakatakasika kwa kuwa pamoja na Mtume *s.a.w.*

Aya 35. *Latiif.* Neno hili tumelifasiri "Mpole," na pia maana yake ni "Mjuzi wa visivyoonekana" (Mufradat).

Aya 36. Katika malipo ya vitendo wanawake na wanaume wote watalipwa sawasawa . Uislamu katika mambo ya dini umeweka usawa baina ya wanaume na wanawake.

وَّالذّٰكِرٰتِ ۙ اَعَدَّ اللّٰهُ لَهُمْ مَّغْفِرَةً وَّاَجْرًا عَظِيْمًا ﴿٣٥﴾

wanawake wanaolinda tupu zao, na wanaume wanaomtaja Allah kwa wingi na wanawake wanaomtaja - Allah Amewaandalia msamaha na ujira mkubwa.

وَمَا كَانَ لِمُؤْمِنٍ وَّلَا مُؤْمِنَةٍ اِذَا قَضَى اللّٰهُ وَرَسُوْلُهٗۤ اَمْرًا اَنْ يَّكُوْنَ لَهُمُ الْخِيَرَةُ مِنْ اَمْرِهِمْ ؕ وَمَنْ يَّعْصِ اللّٰهَ وَرَسُوْلَهٗ فَقَدْ ضَلَّ ضَلٰلًا مُّبِيْنًا ﴿٣٦﴾

37. Haiwi kwa mwanamume aliyeamini wala kwa mwanamke aliyeamini, Allah na Mtume Wake wanapokata shauri, wawe na hiari katika shauri lao. Na mwenye kumwasi Allah na Mtume Wake, hakika amepotea upotevu ulio wazi.

وَاِذْ تَقُوْلُ لِلَّذِيْۤ اَنْعَمَ اللّٰهُ عَلَيْهِ وَاَنْعَمْتَ عَلَيْهِ اَمْسِكْ عَلَيْكَ زَوْجَكَ وَاتَّقِ اللّٰهَ وَتُخْفِيْ فِيْ نَفْسِكَ مَا اللّٰهُ مُبْدِيْهِ وَتَخْشَى النَّاسَ ۚ وَاللّٰهُ اَحَقُّ اَنْ تَخْشٰىهُ ؕ فَلَمَّا قَضٰى زَيْدٌ مِّنْهَا وَطَرًا زَوَّجْنٰكَهَا لِكَيْ لَا يَكُوْنَ عَلَى الْمُؤْمِنِيْنَ حَرَجٌ فِيْۤ اَزْوَاجِ اَدْعِيَآئِهِمْ اِذَا قَضَوْا مِنْهُنَّ وَطَرًا ؕ وَكَانَ اَمْرُ اللّٰهِ مَفْعُوْلًا ﴿٣٨﴾

38. Na ulipomwambia yule ambaye Allah Amemneemesha na (pia) wewe umemneemesha shikamana na mkeo na umche Allah; na ukasitiri katika nafsi yako aliyotaka Allah kuyatoa, na ukawachelea watu, hali Allah ndiye Mwenye haki zaidi umchelee. Basi Zaid alipomaliza haja yake kwa (mwanamke) yule (na kumpa talaka), Tulikuozaye ili isiwe taabu kwa waaminio kuwaoa wake wa wana wao wa kupanga wanapomaliza haja nao (kwa kutalakiana). Na amri ya Allah ni yenye kutekelezwa.

Aya 37. Karibu mufasirina wote wanakubaliana ya kuwa Aya hii ilishuka wakati Mtume *s.a.w.* alipotoa shauri kwa nduguze kuwa binti yao Zainab bint Jahsh aolewe na Zaid bin Harith.

Zainab alikuwa binti wa shangazi wa Mtume *s.a.w.* aitwaye Umeima bint Abdul Muttalib, mtoto wa ukoo mtukufu wa Kikureish. Zaid alikuwa mtu aliyekuja Makka hali yu mtumwa ingawa Mtume alimpa uhuru na kumpanga utoto.

Zainab na kaka yake hawakupenda shauri hili ya kwamba mtu mwenye heshima kama Zainab aolewe na mtu ambaye alikuwa mtumwa. Wao walimwomba Mtume mwenyewe amwoe Zainab. Lakini Mtume kwa kutaka kuondoa fikira za watu kujiona ubora wa kabila, akazidi kuwasihi wakubali aolewe na Zaid. Amri ya Allah iliyomo katika Aya hii ikatia nguvu shauri la Mtume; na Zainab na kaka yake wakakubali aolewe na Zaid.

Aya 38. Mtu ambaye Allah na Mtume wamemneemesha ni Zaid bin Harith, wa kabila la Kalb, ambaye katika utoto wake alitekwa na akauzwa Makka, na Bibi Khadija akapewaye kuwa zawadi na jamaa yake, naye akamtoa zawadi kumpa Mtume *s.a.w.* Mtume

akampa uungwana na akampanga utoto. Wakatokea kupendana sana, hata babaye Zaid aliposikia kuwa mwanawe yuko Makka alikuja kutaka kumkomboa. Mtume s.a.w. akasema, Zaid yu huru ana hiari kuondoka pamoja nanyi. Lakini Zaid alimpenda mno Mtume na hakutaka kuondoka ingawa wazee wake walimsihi sana. Basi Mungu kumneemesha Zaid ni kumpa Uislamu na Mtume kumneemesha ni kumpa uungwana na kumfanyia shauri aoe binti wa shangazi yake.

Shikamana na mkeo na umche Mungu. Zaid na Zainab walipokwisha kuwa mke na mume, Zaid alianza kuona wasiwasi. Ingawa Zainab alikuwa hasemi neno, lakini Zaid akaanza kufikiria ya kuwa Zainab bado anajiona ni bora kuliko yeye. Upande mwingine Zaid binafsi yake akijiona mdogo na ya kuwa yeye si fani ya bibi mtukufu kama Zainab. Fikira hii ilikuwa ikikua kila siku hata ikaleta kutosikilizana kwingi nyumbani mwao. Basi Zaid alifika kwa Mtume akashtaki ya kuwa Zainab anamnyanyasa na pia akasema Zainab anasema naye kwa ukali. (Hadithi inayosimuliwa na Bibi Aisha baadaye, inaonyesha kuwa Zainab hata nyumbani kwa Mtume alikuwa na tabia ya ukali ambayo alikuwa anafanya bidii kuizuia. Ilikuwa ni tabia yake tu - Muslim, jalada 2). Zaid akaomba apewe ruhusa kumpa talaka Zainab. Jambo hili lilimsikitisha sana Mtume, akaona ya kwamba juhudi ya Zaid ya kujenga masikilizano imepungua. Basi Mtume s.a.w. akamwambia Zaid, "Kaa na mkeo na umche Mungu" (Bukhari), asaa Mungu atakusaidia taabu uzionazo zitakuondokea.

Na ukasitiri, katika nafsi yako aliyotaka Mungu kuyatoa. Zaid alikubali nasaha ya Mtume na akajaribu kujishikiza kukaa na mkewe; lakini donda alilokuwa nalo moyoni halikuonyesha alama ya kupona. Hitililafu zake na mkewe zikashika sana hata akatoa talaka kumwacha mkewe.

Jambo hili la kuachwa Zainab lilikuwa ni aibu sana kwa ajili ya bibi huyu. Tokea hapo Waarabu walikuwa hawaoi wanawake walioachwa na waliwadharau sana. Na ilikuwa ndiyo mara ya kwanza mwanamke wa ukoo mtukufu kuachwa na mtu aliyekuwa mtumwa, wacha mbali jambo la kuolewa naye. Hii ilikuwa ni fedheha dhahiri kwa ajili ya Zainab. Zainab akahisi ya kuwa asingeaibishwa namna hii kama si tashtiti za Mtume aliyekazania aolewe na Zaid!

Kumsaidia Zainab na kumpoza huzuni yake ilikuwa mahali pake aolewe katika nyumba tukufu kabisa. Mwenyezi Mungu akatia wazo katika moyo wa Mtume ya kuwa yeye ndiye angestahili kumwoa Zainab ili kuzima majonzi yake na kupoza chuki ya ndugu wengine wa Zainab. Upande, Mtume anaogopa akimwoa Zainab watu watasema ya kuwa amemwoa mkwewe aliyekuwa mke wa mwanawe wa kupanga. Jambo hili Mtume akalizuia rohoni asitake kulitoa ya kwamba yeye amwoe Zainab. Kwa sababu hii Mungu anasema, *Ukastiri katika nafsi yako aliyotaka Mungu kuyatoa,* yaani Mungu alitaka jambo hili litendeke, hivyo ilikuwa kazi bure Mtume kulificha rohoni.

Allah alitaka kutimiza mambo matatu katika jambo hili: (1) uchungu wa Zainab uishe; (2) desturi ya kuacha kuoa wanawake walioachwa ifutike; (3) ijulikane kwa Waislamu kuwa desturi ya kupanga watoto haina maana na ifutike kabisa; kama asemavyo Allah, *Alipokwisha maliza haja yake na mwanamke yule (yaani kumpa talaka) Tulikuoza ili isiwe taabu kwa waaminio kuwaoa wake wa wana wao wa kupanga wanapomaliza haja nao. Na amri ya Allah iwe yenye kutekelezwa.*

Baada ya Wahyi huu Mtume *s.a.w.* akapeleka ujumbe (Muslim) wa kumwoa Zainab. Zainab na kaka yake wakakubali. Kaka yake, Abu Ahmad bin Jahsh, akawa walii na akamwoza kwa mahari ya dirham 400/- (Sirat Ibn Hisham).

Kuna watu wanaosema ya kuwa Mtume *s.a.w.* alimwona Zainab nyumbani mwa Zaid na uzuri wake ukamwathiri sana, na akasema: *Subhaanallaah muqallibul quluub,* yaani: "Utakatifu ni wa Mungu ambaye huipindua mioyo," uzuri siyo huu? Zainab aliposikia maneno haya ya Mtume *s.a.w.* akamwambia mumewe Zaid kuwa Mtume ameniona na amesifia uzuri wangu. Hapo Zaid akajua kuwa Mtume anapenda Zainab awe mkewe, basi akamwacha, na Mtume *s.a.w.* akamwoa.

مَا كَانَ عَلَى النَّبِيِّ مِنْ حَرَجٍ فِيْمَا فَرَضَ
اللّٰهُ لَهٗ ؕ سُنَّةَ اللّٰهِ فِي الَّذِيْنَ خَلَوْا مِنْ قَبْلُ ؕ
وَكَانَ اَمْرُ اللّٰهِ قَدَرًا مَّقْدُوْرَا ۙ﴿۳۹﴾

39. Si kosa kwa Nabii katika yale ambayo Allah Amemlazimisha: ndiyo kawaida ya Allah kwa wale waliopita zamani; na amri ya Allah ni kipimo kilichokadiriwa.

الَّذِيْنَ يُبَلِّغُوْنَ رِسٰلٰتِ اللّٰهِ وَيَخْشَوْنَهٗ
وَلَا يَخْشَوْنَ اَحَدًا اِلَّا اللّٰهَ ؕ وَكَفٰى بِاللّٰهِ
حَسِيْبًا ﴿۴۰﴾

40. Wale wanaofikisha risala za Allah na kumwogopa Yeye wala hawamwogopi (ye yote) isipokuwa Allah; na Allah ndiye Atoshaye kuhesabu.

مَا كَانَ مُحَمَّدٌ اَبَآ اَحَدٍ مِّنْ رِّجَالِكُمْ
وَلٰكِنْ رَّسُوْلَ اللّٰهِ وَخَاتَمَ النَّبِيّٖنَ ؕ
وَكَانَ اللّٰهُ بِكُلِّ شَيْءٍ عَلِيْمًا ﴿۴۱﴾ ع

41. Muhammad si baba ya ye yote katika wanaume wenu, bali yeye ni Mtume wa Allah na Muhuri wa Manabii. Na Allah ndiye Ajuaye kila kitu.

Msingi wa porojo hili ni dhaifu kabisa. Wanasema ati Mtume *s.a.w.* alimwona Zainab ndipo akamtamani. Zainab hakuwa mgeni kwa Mtume. Alikuwa binti wa Shangazi yake hasa na walikuwa wanafahamiana sana. Wakati huo amri ya wanawake kuvaa hijabu ilikuwa haijashuka. Mbona asimtamani hapo? Zainab mwenyewe na kaka yake walitaka Mtume mwenyewe amwoe kabla hajaolewa na Zaid, lakini Mtume akakataa, na akawasihi sana wampose Zaid. Kama Zainab alikuwa mzuri wa kumshtusha Mtume s.a.w., kwa nini asikubali kumwoa kabla hajaguswa na mwanamume mwingine? Ndoa hii ilimfanya Zainab aone fahari maana aliolewa kwa amri ya Allah na hivyo alikuwa na uso mbele ya wake wenziwe. Kama angeolewa kwa sababu ya kutamaniwa vile na Mtume, mwenyewe angefanya shaka moyoni mwake juu ya usafi na utawa wa Mtume.

Ni jambo la kusikitisha sana kuona ya kuwa hata baadhi ya wafasiri wa Kiislamu wamekubali uwongo huu uliotungwa na Waakidi bila ushahidi wo wote. Uwongo huu ni mchafu kabisa na haupatani kamwe na sifa za utakatifu na unyofu wa yule Mfalme wa Manabii Muhammad *s.a.w.*

Aya 41. Muhammad si baba ya ye yote, yaani si baba wa damu. Wakeze wameitwa mama za waaminio kwa sababu ya heshima tu, siyo kwamba wamekuwa kama mama wa damu wanaoweza kurithi.

Katika mwaka wa tano wa Hijra Mtume *s.a.w.* alipomwoa Zainab makafiri walianza kupiga kelele ya kuwa Mtume s.a.w. ameoa mwanamke aliyekuwa mke wa mwanawe. Basi Allah aliteremsha Aya hii kuwajibu ya kwamba Mtume *s.a.w.* hana mwana wa damu kwa hiyo upinzani huo uko mbali naye.

Khaatamannabiyyiin, "Muhuri wa Manabii." Neno Khaatam katika lugha ya Kiarabu lina maana ya "Muhuri." Inasimuliwa ya kuwa siku moja Mtume *s.a.w.* alinuia kuandika barua za kuwabashiri wafalme, na masahaba wakasema ya kwamba Wafalme wa Kiajemi hawapokei barua mpaka iwe na muhuri wa mwandikaji. Mtume *s.a.w.* alitengeneza *khaatam* na juu yake

yakaandikwa maneno: Muhammad Mtume wa Mungu (Bukhari jalada 1; Muslim *Kitaab-ul-Libaas*). Hadithi hii inaonyesha ya kuwa kazi kubwa ya muhuri ni kuhakikisha. Mtume *s.a.w.* alipoitwa na Allah *Khaatamannabiyyiin* (Muhuri wa Manabii), ni kudhihirisha ya kuwa bila muhuri wa Mtume *s.a.w.* ukweli wa Nabii ye yote hautathibitika; yaani Mtume *s.a.w*. amepewa cheo cha kusadikisha. Asingefika yeye ukweli na utakatifu wao ungekuwa katika hali ya giza.

Tena, kama muhuri unapigwa juu ya kitu, chapa inaonekana juu ya kitu hicho. Hivyo Mtume *s.a.w.* alipoitwa "Muhuri wa Manabii" ilitabiriwa ya kuwa kama muhuri wake utapigwa unabii utapatikana. Yaani utakatifu wake umekamilika hata umefika kwenye cheo cha kutoa kuwapa wengine daraja ya unabii kwa kupigwa muhuri wake. Kwa mujibu wa maana hii Seyidna Ahmad amesema, "Allah amempa Mtume *s.a.w.* muhuri, yaani amepewa ili awape wengine sifa ya unabii, na hakuna Nabii mwingine aliyepewa muhuri namna hii. Kwa sababu hii ameitwa *Khaatamannabiyyiin,* maana kumfuata kunatoa sifa za unabii, na nguvu yake ya utawa inamfanya mtu awe Nabii; na hakuna Nabii mwingine aliyepata nguvu hii ya utakatifu." (Haqiiqatulwahyi uk. 97).

Neno *khaatam* pia lina maana ya "pete." Imesimuliwa na sahaba mmoja ya kuwa Mtume *s.a.w.* alikataza kutumia vyombo vya fedha na *khaatam* (pete) ya dhahabu na nguo za hariri (Bukhari jalada 1, uk. 143). Katika hadithi nyingine imesimuliwa ya kuwa Mtume *s.a.w.* alimwambia mtu mmoja aliyekuwa na pete ya chuma *(khaataman min hadiidin)*, "Imekuwaje nakuona umevaa pete ya chuma iliyo pambo la makafiri na la watu wa Jahanamu?"

Ni dhahiri katika hadithi hizi mbili ya kuwa neno la *khaatam* limekuwa na maana ya pete. Mtume *s.a.w*. alitumia pete ya fedha na akawaruhusu Waislamu kutumia pete ya fedha kwa wanaume na ya dhahabu pia kwa wanawake; na kila mara alitumia neno la *khaatam* kwa pete.

Pete hutumiwa kwa ajili ya mapambo. Mtume *s.a.w.* kuitwa *Khaatamannabiyyiin* (Pete ya Manabii), Allah ameonyesha ya kuwa Mtume *s.a.w.* amefanywa pambo kwa ajili ya Manabii. Kama Mtume Muhammad *s.a.w*. asingefika duniani, Manabii wasingepata kupambwa, kwa kuwa wamepewa sifa mbaya katika vitabu vya Mayahudi na Wakristo kama tulivyoeleza mahali pengine humu katika tafsiri hii. Hivyo Mtume *s.a.w.* kwa kutangaza heshima na utakatifu wa Manabii wote amekuwa sababu ya uzuri na mapambo kwa ajili yao. Kama watu wapatavyo kupambwa kwa kuvaa pete ndivyo ambavyo Mtume *s.a.w.* amekuwa Pete kwa ajili ya Manabii.

Katika Taafsiri Fat'hul Bayan imesemwa, "Mtume *s.a.w.* amekuwa *Khaatam* (Pete) kwa ajili ya Manabii, na amekuwa pambo kwa ajili yao kwa kuwa yu mmoja wao" (Jalada 7). Katika kitabu kingine cha kamusi mmeandikwa chini ya neno *khaatam,* "Na Muhammad ni *Khaatamannabiyyin* (kwa *te* yenye *fat'ha* katika *khaatam*) kwa maana ya mapambo. Maana hii imechukuliwa katika neno *khaatam* (pete) ambayo ni pambo kwa anayeitumia" (Majma'ul-Bahrain). Zurkani ameandika chini ya neno la *khaatam* maana ya "mbora" kwa kuumbwa na kwa tabia, maana Mtume *s.a.w.* ni pambo la Manabii kama ilivyo pete pambo la kidole.

Kadhalika kama vile pete hukizunguka kidole , Mtume *s.a.w.* amewazunguka Manabii wote; yaani sifa mbalimbali za Manabii mbalimbali zimekusanyika zote kwa Mtume Muhammad *s.a.w.*

Ukiichungua lugha ya Kiarabu utaona ya kuwa neno *khaatam* pia lina maana ya "ubora." Neno *khaatam* linapokuwa *mudhaaf* (kiungo) kwenye ismu ya wingi, basi ismu ile inakuwa *mudhaaf ilaihi* (yenye kumiliki) na hapo neno *khaatam* linakuwa na maana ya *ubora.*

Kwa mfano, *Khaatamul mufassiriin* maana yake ni "mbora wa wanaofasiri." *Khaatamul Muhaajiriin* ni "Mbora wa Wanaohama." (Kanzul Ummal jalada 6, uk. 31). *Khaatamul Auliyaa* ni "Mbora wa Mawalii" (Tafsiir Saafiy). *Khaatamush-Shu'araa* ni "Mbora wa Watunga mashairi" (Waafiyatul Ayyan li Ibni Khalkan); n.k.w.

Hivyo kwa kanuni hii ya nahau ya Kiarabu, neno *Khaatamannabiyyiin* litatafsiriwa "Mbora wa Manabii," wala hakuna mfano hata mmoja katika lugha ya Kiarabu ulio kinyume na kanuni hii. Imam Fakhrud-Din-Razi ameandika kueleza habari za maendeleo ya mwanadamu na amesema, "Allah aliwapa wanadamu akili, na akatia katika roho zao nuru ya busara na sifa ya

kuongoza. Hivyo wenye cheo hiki wamepata mambo manne ya heshima:-

"(1) Kuwako; (2) uzima; (3) uwezo na (4) akili. Na akili ni *khaatamul-kulli* (bora kuliko vyote), na *khaatam* lazima liwe na maana ya ubora. Je huoni Mtume *s.a.w.* alipokuwa *Khaatamannabiyyiin* amekuwa Mbora wa Manabii, na mwanadamu alipokuwa *Khaatamulmakhluuqaat* amekuwa mbora wa viumbe? Hivyo akili ilipokuwa *Khaatamul-khul'a* imekuwa bora na yenye sifa kamili kuliko sifa na heshima nyingine zinazotoka kwa Allah" (Tafsir Kabir, jalada 6).

Wako wanazuoni wengine waliosema ya kuwa neno *Khaatamannabiyyiin* maana yake ni "Nabii wa mwisho wa kuleta Sheria." Imam Ali Al-Qari amesema, *Khaatamannabiyyiin* maana yake ni kwamba hatakuja baada ya Mtume s.a.w. Nabii atakayevunja sheria yake na atakayekuwa si mfuasi wake" (Maudhu'at Kabir).

Sufi mkubwa Sheikh-ul-Akbra Muhyu-d-Din Ibni Arabi amesema, "Utume uliokatika kwa kufika Mtume *s.a.w.* ni utume wa Sheria, siyo cheo cha utume. Hivyo hakutakuwa na sheria itakayovunja Sheria ya Mtume Muhammad *s.a.w.* na hakutakuwa na sheria itakayozidisha hukumu yo yote katika Sheria yake. Hii ndiyo maana ya Hadithi ya Mtume *s.a.w.* aliposema, "Hakika utume na unabii umekatika, basi hakuna Mtume wala Nabii baada yangu" yaani hakutakuwa na Nabii atakayekuwa kinyume cha Sheria yangu, bali atakuwa chini ya hukumu ya Sheria yangu" (Futuhat Makkiyya jalada 2, uk. 3). Tena mcha-Mungu huyo amesema, "Utume umekatika kwa maana ya kuwa hataweza kuja Mtume wa kuleta sheria ya kuvunja Sheria ya Mtume Muhammad *s.a.w.* Utume utaendelea mpaka siku ya Kiyama" (futuhat Makkiyya 2, mlango 73).

Hadhrat Seyid Abdul Karim Jilani amesema, "Hukumu ya unabii wa sheria imekatika baada ya Mtume *s.a.w.* hivyo amekuwa *Khaatamannabiyyiin"* (Al-Insaanul-Kamil, mlango 36).

Bibi Aisha, mke wa Mtume *s.a.w.* alisema, "Semeni yeye ni *Khaatamannabiyyiin* lakini msiseme hakuna Nabii baada yake" (Tafsir Durri Manthur).

Imam Abdul Wahhaab Shaarani amesema, "Utume haukufungwa kabisa, Mtume ambaye hawezi kuja ni yule wa kuleta Sheria" (Alyawaaqiit wal Jawaahir).

Imam Muhammad Tahir amesema, "Mradi wa *Laa nabiyya ba'adi* ni kuwa hatakuja Nabii wa kuvunja Sheria yake" (Takmil Majma'ul Bihar, uk. 85).

Sheikh Muhammad KasimNanutwi, mwanzilishi wa madrasa kubwa ya Kisunni ya Deoband, alisema, "Kwa mfano, kama Nabii mwingine aje baada ya Mtume *s.a.w.* haitakuwa kinyume cha *Khatmayyat-i-Muhammad"* (Tahdhirun-Naas, uk. 28).

Seyidna Ahmad (*'alaihissalaam*) amesema, "Mtume *s.a.w.* amepewa heshima maalum ya kuwa yeye ni *Khaatamul-Anbiya* kwa maana ya kuwa sifa zote za unabii zimekwisha timia katika dhati yake, na ya kwamba hakutakuwa Nabii mwingine baada yake atakayeleta sheria mpya, wala hakutakuwa Nabii baada yake atakayekuwa nje ya umati wake, bali kila anayepata baraka za kuzungumza na Allah kwa hakika anapata katika kipawa cha Mtume *s.a.w.*, na kwa kumfuata; hivyo anaitwa Nabii mfuasi wala haitwi Nabii aliyepokea utume moja kwa moja kutoka kwa Allah" (Tatimma Chashma Ma'arifat).

Kwa neno zima, maneno *Khaatamannabiyyin* yameteremshwa kwa kumsifu Mtume *s.a.w.* na hivyo yanatakiwa kufasiriwa kwa maana ihakikishayo ubora wake; maana kutoa tafsiri nyingine ghairi ya hizo haikubaliwi na lugha wala haikubaliwi na Qur'an yanyewe, haikubaliwi na Hadithi wala haikubaliwi na wanazuoni watawa. Kwa sababu hii mwanachuoni mkubwa, Sheikh Muhammad Kasim Nanutwi akasema: "Watu wasio na maarifa wanafahamu ya kuwa Mtume *s.a.w.* ni *Khaatam* kwa maana ya kuwa amekuja mwisho wa Manabii wote kwa majira, na hivyo amekuwa mwisho wa Manabii wote. Lakini wenye maarifa wanajua ya kuwa kuja mbele au nyuma katika zama si jambo la heshima au ubora, na katika halii hii kutamka *Khaatamannabiyyiin* kuwa sifa nzuri itakuwaje sawa?" (Tahdhir-un-Naas).

Hata Mtume *s.a.w.* mwenyewe amevunja mawazo ya namna hii aliposema wakati alipofariki mtoto wake Ibrahimu, miaka minne baada ya kushuka Aya *Khaatamannabiyyiin* katika mwaka wa tisa baada ya kuhama, "Angeishi Ibrahimu angekuwa Nabii mkweli" (Ibni Majah).

FUNGU 6

يَاَيُّهَا الَّذِيْنَ اٰمَنُوا اذْكُرُوا اللّٰهَ ذِكْرًا كَثِيْرًا ﴿٤٢﴾

42. Enyi mlioamini, Mkumbukeni Allah kwa wingi,

وَّسَبِّحُوْهُ بُكْرَةً وَّاَصِيْلًا ﴿٤٣﴾

43. Na Mtukuzeni asubuhi na jioni.

هُوَ الَّذِيْ يُصَلِّيْ عَلَيْكُمْ وَمَلٰٓئِكَتُهٗ لِيُخْرِجَكُمْ مِّنَ الظُّلُمٰتِ اِلَى النُّوْرِ ؕ وَكَانَ بِالْمُؤْمِنِيْنَ رَحِيْمًا ﴿٤٤﴾

44. Yeye ndiye Anayewarehemuni na Malaika Wake, ili kuwatoeni katika giza kuwapelekeni kwenye nuru, naye ni Mrehemevu kwa waaminio.

تَحِيَّتُهُمْ يَوْمَ يَلْقَوْنَهٗ سَلٰمٌ ۚ وَاَعَدَّ لَهُمْ اَجْرًا كَرِيْمًا ﴿٤٥﴾

45. Maamkio yao siku ya kukutana naye yatakuwa, Amani; na Amewaandalia malipo yenye heshima.

يٰٓاَيُّهَا النَّبِيُّ اِنَّاۤ اَرْسَلْنٰكَ شَاهِدًا وَّمُبَشِّرًا وَّنَذِيْرًا ﴿٤٦﴾

46. Ewe Nabii, kwa yakini Sisi Tumekutuma (ili uwe) shahidi na Mtoaji wa habari njema, na Mwonyaji,

وَّدَاعِيًا اِلَى اللّٰهِ بِاِذْنِهٖ وَسِرَاجًا مُّنِيْرًا ﴿٤٧﴾

47. Na mwitaji (wa watu) kwa Allah, kwa idhini Yake, na jua litoalo nuru.

وَبَشِّرِ الْمُؤْمِنِيْنَ بِاَنَّ لَهُمْ مِّنَ اللّٰهِ فَضْلًا كَبِيْرًا ﴿٤٨﴾

48. Na wape habari njema waaminio ya kwamba wana fadhili kubwa itokayo kwa Allah.

وَلَا تُطِعِ الْكٰفِرِيْنَ وَالْمُنٰفِقِيْنَ وَدَعْ اَذٰىهُمْ وَتَوَكَّلْ عَلَى اللّٰهِ ؕ وَكَفٰى بِاللّٰهِ وَكِيْلًا ﴿٤٩﴾

49. Na usiwatii makafiri na wanafiki, wala usijali udhia wao, na tegemea kwa Allah; na Allah Anatosha kuwa Mlinzi.

يٰٓاَيُّهَا الَّذِيْنَ اٰمَنُوْۤا اِذَا نَكَحْتُمُ الْمُؤْمِنٰتِ ثُمَّ طَلَّقْتُمُوْهُنَّ مِنْ قَبْلِ اَنْ تَمَسُّوْهُنَّ فَمَا لَكُمْ عَلَيْهِنَّ مِنْ عِدَّةٍ تَعْتَدُّوْنَهَا ۚ فَمَتِّعُوْهُنَّ وَسَرِّحُوْهُنَّ سَرَاحًا جَمِيْلًا ﴿٥٠﴾

50. Enyi mlioamini! Mtakapowaoa waaminio, kisha mkawapa talaka kabla ya kuwagusa, basi hamna eda juu yao mtakayohesabu. Na wapeni matumizi na kuwasindikiza msindikizo mwema.

Basi ingekuwa muradi katika Aya ni kwamba Mtume Muhammad *s.a.w.* ni wa mwisho na haji tena baada yake Nabii, Mtume angethubutuje kusema, "Kama Ibrahimu angeishi angekuwa Nabii"?

Aya 50. *Wapeni matumizi.* Kama hesabu ya mahari ilikwisha katwa na mwanamke ameachwa kabla ya kuingiliwa, atapewa nusu ya mahari na hatakuwa na eda. Lakini kama mahari hayakuwekwa wakati wa kufunga ndoa, basi atapewa cho chote na kushindikizwa kwa wema.

51. Ewe Nabii! Hakika Tumekuhalalishia wake zako ambao uliwapa mahari yao, na (wanawake) uliowatamalaki mkono wako wa kuume katika wale Aliokupa Allah, na mabinti wa amu yako na mabinti wa shangazi zako, na mabinti wa mjomba wako na mabinti wa dada ya mama yako, waliohama pamoja nawe, na mwanamke mwaminio akijitoa mwenyewe kwa Nabii, na kama Nabii akitaka kumwoa: ni halali kwako tu si kwa waaminio wengine. Bila shaka Tumekwishajua Tuliyowafaradhishia katika wake zao, na iliyowatamalaki mikono yao ya kuume, ili isiwe dhiki kwako; na Allah ni Msamehevu, Mrehemevu.

52. Umwache umtakaye miongoni mwao, na kumkaribisha umtakaye, na kama ukimtaka tena yule uliyekwisha mtenga, basi si vibaya kwako; hii itakuwa karibu zaidi katika kuyaburudisha macho yao na wala wasihuzunike, na wawe radhi juu ya kile unachowapa, wao wote. Na Allah Anayajua yaliyomo mioyoni mwenu, na Allah ni Ajuaye, Mpole.

53. Baada ya hawa si halali kwako (kuoa) wanawake (wengine) wala (si halali) kuwabadilisha kwa wake

يٰۤاَيُّهَا النَّبِيُّ اِنَّاۤ اَحْلَلْنَا لَكَ اَزْوَاجَكَ
الّٰتِيْۤ اٰتَيْتَ اُجُوْرَهُنَّ وَ مَا مَلَكَتْ
يَمِيْنُكَ مِمَّاۤ اَفَآءَ اللّٰهُ عَلَيْكَ وَبَنٰتِ
عَمِّكَ وَبَنٰتِ عَمّٰتِكَ وَ بَنٰتِ خَالِكَ
وَ بَنٰتِ خٰلٰتِكَ الّٰتِيْ هَاجَرْنَ مَعَكَ ۫
وَامْرَاَةً مُّؤْمِنَةً اِنْ وَّهَبَتْ نَفْسَهَا لِلنَّبِيِّ
اِنْ اَرَادَ النَّبِيُّ اَنْ يَّسْتَنْكِحَهَا ۗ خَالِصَةً لَّكَ
مِنْ دُوْنِ الْمُؤْمِنِيْنَ ؕ قَدْ عَلِمْنَا مَا فَرَضْنَا
عَلَيْهِمْ فِيْۤ اَزْوَاجِهِمْ وَ مَا مَلَكَتْ
اَيْمَانُهُمْ لِكَيْلَا يَكُوْنَ عَلَيْكَ حَرَجٌ ؕ
وَكَانَ اللّٰهُ غَفُوْرًا رَّحِيْمًا ۝٥١
تُرْجِيْ مَنْ تَشَآءُ مِنْهُنَّ وَ تُـْٔوِيْۤ اِلَيْكَ
مَنْ تَشَآءُ ؕ وَ مَنِ ابْتَغَيْتَ مِمَّنْ عَزَلْتَ
فَلَا جُنَاحَ عَلَيْكَ ؕ ذٰلِكَ اَدْنٰۤى اَنْ تَقَرَّ
اَعْيُنُهُنَّ وَ لَا يَحْزَنَّ وَ يَرْضَيْنَ
بِمَاۤ اٰتَيْتَهُنَّ كُلُّهُنَّ ؕ وَاللّٰهُ يَعْلَمُ مَا
فِيْ قُلُوْبِكُمْ ؕ وَكَانَ اللّٰهُ عَلِيْمًا حَلِيْمًا ۝٥٢
لَا يَحِلُّ لَكَ النِّسَآءُ مِنْۢ بَعْدُ وَلَاۤ اَنْ تَبَدَّلَ
بِهِنَّ مِنْ اَزْوَاجٍ وَّلَوْ اَعْجَبَكَ حُسْنُهُنَّ

Aya 52. Aya hii isomwe pamoja na Aya 29 na 30. Katika Aya hizi wake wa Mtume walipewa hiyari kukaa pamoja na Mtume ikiwa hawatataka mali na anasa za kidunia, au siyo waende zao. Wao wakachagua kuendelea kuwa wake wa Mtume. Katika Aya hii Mtume naye amepewa hiari kukaa na amtakaye na kumwacha amtakaye kwa kuhusiana na tukio lile. Mtume pia akaona huruma juu yao na akaendelea kuwa mume wao. Ikumbukwe ya kuwa Mtume hakupewa ruhusa kuwaacha wake zake na kuoa wengine. Na upande mwingine Mtume amepewa ruhusa kumwoa bila mahari (Aya 51) mwanamke anayetaka kuolewa naye (anavyofasiri Ima Abu Hanifa), jambo ambalo waaminio wengine hawakuruhusiwa.

إِلَّا مَا مَلَكَتْ يَمِينُكَ ۗ وَكَانَ اللَّهُ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ رَّقِيبًا ﴿٥٢﴾ ع ٦

wengine hata kama uzuri wao ukupendeza, isipokuwa yule uliyemtamalaki mkono wako wa kuume. Na Allah ni Mchungaji wa kila kitu.

FUNGU 7

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا لَا تَدْخُلُوا بُيُوتَ النَّبِيِّ إِلَّا أَنْ يُؤْذَنَ لَكُمْ إِلَىٰ طَعَامٍ غَيْرَ نَاظِرِينَ إِنَاهُ وَلَٰكِنْ إِذَا دُعِيتُمْ فَادْخُلُوا فَإِذَا طَعِمْتُمْ فَانْتَشِرُوا وَلَا مُسْتَأْنِسِينَ لِحَدِيثٍ ۚ إِنَّ ذَٰلِكُمْ كَانَ يُؤْذِي النَّبِيَّ فَيَسْتَحْيِي مِنْكُمْ ۖ وَاللَّهُ لَا يَسْتَحْيِي مِنَ الْحَقِّ ۚ وَإِذَا سَأَلْتُمُوهُنَّ مَتَاعًا فَاسْأَلُوهُنَّ مِنْ وَرَاءِ حِجَابٍ ۚ ذَٰلِكُمْ أَطْهَرُ لِقُلُوبِكُمْ وَقُلُوبِهِنَّ ۚ وَمَا كَانَ لَكُمْ أَنْ تُؤْذُوا رَسُولَ اللَّهِ وَلَا أَنْ تَنْكِحُوا أَزْوَاجَهُ مِنْ بَعْدِهِ أَبَدًا ۚ إِنَّ ذَٰلِكُمْ كَانَ عِنْدَ اللَّهِ عَظِيمًا ﴿٥٣﴾

54. Enyi mlioamini! msiingie nyumba za Nabii ila kama mpewe ruhusa kwenda kula, pasipo (kwenda kaa) kungojea kiive. Lakini mtakapoitwa, basi ingieni; na mnapokwisha kula, tawanyikeni. Wala msishughulike kuzungumza (baada ya kula), maana jambo hili humwudhi Mtume, naye huwaoneeni haya; lakini Allah Haoni haya kusema haki. Nanyi mnapowaomba (wakeze) kitu, basi waombeni nyuma ya pazia. Hayo ni safi kabisa kwa mioyo yenu na kwa mioyo yao. Wala haiwapasini kumwudhi Mtume wa Allah, wala msiwaoe wake zake baada yake abadan. Hakika hilo ni (dhambi) kubwa mbele ya Allah.

إِنْ تُبْدُوا شَيْئًا أَوْ تُخْفُوهُ فَإِنَّ اللَّهَ كَانَ بِكُلِّ شَيْءٍ عَلِيمًا ﴿٥٤﴾

55. Mkidhihirisha cho chote au kukificha, basi hakika Allah Hukijua kila kitu.

لَا جُنَاحَ عَلَيْهِنَّ فِي آبَائِهِنَّ وَلَا أَبْنَائِهِنَّ

56. Si dhambi juu yao katika (kuonana na) baba zao, wala watoto

Aya 54. Mtu anayekaribishwa mahali kwa chakula, anatakiwa afike wakati ule ule alioambiwa. Siyo kwenda kukingoja chakula kinapikwa, maana, namna hii mtu anaonekana mroho na pia mwenyeji wake anakuwa na kazi ya kutengeneza chakula na kazi zingine hawezi kuona vizuri kushughulika na wageni wanaofika wakati asiowatazamia.

Kadhalika baada ya kula si vizuri kukaa na kuzungumza, ili wenye nyumba wawe na nafasi ya kumaliza kazi na haja zao zingine.

(Dhambi) kubwa inayoelezwa hapa ni kumwudhi Mtume na kuoa wake wa Mtume baada ya kufariki kwake. Hii ndiyo adabu kubwa inayofundishwa na dini ya Kiislamu juu ya kuhifadhi heshima ya Mtume na wakeze. Kama wakeze wangeolewa na watu wengine, isingekuwa rahisi kwa watu kwenda pata kwao habari za mambo ya dini waliyojifunza kwa Mtume, heshima yao pia isingejulikana, nao wasingeheshimu madaraka yao.

وَلَآ اِخْوَانِهِنَّ وَلَآ اَبْنَآءِ اِخْوَانِهِنَّ وَلَآ اَبْنَآءِ اَخَوٰتِهِنَّ وَلَا نِسَآئِهِنَّ وَلَا مَا مَلَكَتْ اَيْمَانُهُنَّ ۚ وَاتَّقِيْنَ اللّٰهَ ۭ اِنَّ اللّٰهَ كَانَ عَلٰي كُلِّ شَيْءٍ شَهِيْدًا ۝۵۵

wao, wala kaka zao, wala wana wa kaka zao, wala wana wa dada zao, wala wanawake waaminio, wala wale iliyowatamalaki mikono yao ya kuume. Na Mwogopeni Allah (enyi wanawake); bila shaka Allah ni Shahidi juu ya kila kitu.

اِنَّ اللّٰهَ وَمَلٰۗىِٕكَتَهٗ يُصَلُّوْنَ عَلَي النَّبِيِّ ۭ يٰٓاَيُّهَا الَّذِيْنَ اٰمَنُوْا صَلُّوْا عَلَيْهِ وَسَلِّمُوْا تَسْلِيْمًا ۝۵۶

57. Hakika Allah na Malaika Wake humrehemu Mtume; enyi mlioamini, msalieni (Mtume) na mwombeeni amani.

اِنَّ الَّذِيْنَ يُؤْذُوْنَ اللّٰهَ وَرَسُوْلَهٗ لَعَنَهُمُ اللّٰهُ فِي الدُّنْيَا وَالْاٰخِرَةِ وَاَعَدَّ لَهُمْ عَذَابًا مُّهِيْنًا ۝۵۷

58. Kwa yakini wale wanaomwudhi Allah na Mtume Wake, Allah Amewalaani katika dunia na Akhera, na Amewaandalia adhabu ifedheheshayo.

وَالَّذِيْنَ يُؤْذُوْنَ الْمُؤْمِنِيْنَ وَالْمُؤْمِنٰتِ بِغَيْرِ مَا اكْتَسَبُوْا فَقَدِ احْتَمَلُوْا بُهْتَانًا وَّاِثْمًا مُّبِيْنًا ۝۵۸ ع

59. Na wale wanaowaudhi wanaume waaminio na wanawake waaminio pasipo wao kufanya kosa lo lote, bila shaka wamebeba masingizio na dhambi iliyo dhahiri.

FUNGU 8

يٰٓاَيُّهَا النَّبِيُّ قُلْ لِّاَزْوَاجِكَ وَبَنٰتِكَ وَنِسَاۗءِ الْمُؤْمِنِيْنَ يُدْنِيْنَ عَلَيْهِنَّ مِنْ جَلَابِيْبِهِنَّ ۭ ذٰلِكَ اَدْنٰٓى اَنْ يُّعْرَفْنَ فَلَا يُؤْذَيْنَ ۭ وَكَانَ اللّٰهُ غَفُوْرًا رَّحِيْمًا ۝۵۹

60. Ewe Nabii, waambie wake zako, na mabinti zako, na wanawake wa waaminio, wateremshe juu yao shungi zao. Hivyo inaelekea zaidi wajulikane na wasiudhiwe. Na Allah ni Msamehevu, Mrehemevu.

Aya 57. *Sala* maana yake ni, baraka, rehema, salama na cheo kikubwa. Hivyo Allah na Malaika kumsalia Mtume ni kumteremshia baraka na rehema na cheo na salama; na watu kumsalia Mtume, mradi wake ni kumwombea baraka na rehema.

Aya 58. *Amewalaani,* yaani anawaweka mbali na rehema Zake (Baidhawi).

Aya 60. Aya hii ya wanawake kujifunika shungi nyuso zao imeshuka baada ya kuolewa Zainab bint Jahsh na Mtume *s.a.w.*

Wateremshe juu yao shungi zao, yaani shungi ziteremshwe hata zifunike nyuso. Katika tafsiri ya Aya hii imesemwa, "Wafunike nyuso zao na miili yao kwa nguo kubwa watakapotoka nje kwa haja" (Baidhawi). Ibn Abbas anasema, "Allah amewaamrisha wanawake Waislamu watakapotoka nje kwa haja waangushe nguo kutoka kichwani na kufunika nyuso zao" (Tafsir Ibn Jarir).

61. Kama wanafiki, na wale wenye maradhi mioyoni mwao, na watangazao habari za uongo mjini hawataacha (tabia hiyo) kwa yakini Tutakufanya wewe usimame dhidi yao (kuwaadhibu); kisha hawataweza kuishi jirani yako ila kwa muda kidogo tu.

لَئِنْ لَّمْ يَنْتَهِ الْمُنٰفِقُوْنَ وَالَّذِيْنَ فِيْ قُلُوْبِهِمْ مَّرَضٌ وَّالْمُرْجِفُوْنَ فِي الْمَدِيْنَةِ لَنُغْرِيَنَّكَ بِهِمْ ثُمَّ لَا يُجَاوِرُوْنَكَ فِيْهَآ اِلَّا قَلِيْلًا ﴿٦١﴾

62. Maluuni (hao); po pote waonekanapo wakamatwe na wauawe kabisa.

مَّلْعُوْنِيْنَ ۚ اَيْنَمَا ثُقِفُوْٓا اُخِذُوْا وَقُتِّلُوْا تَقْتِيْلًا ﴿٦٢﴾

63. Hii ni kawaida ya Allah iliyokuwa kwa wale waliopita zamani; wala hutapata mabadiliko katika kawaida ya Allah.

سُنَّةَ اللّٰهِ فِي الَّذِيْنَ خَلَوْا مِنْ قَبْلُ ۚ وَلَنْ تَجِدَ لِسُنَّةِ اللّٰهِ تَبْدِيْلًا ﴿٦٣﴾

64. Watu wanakuuliza habari za saa ile. Sema: Elimu yake iko kwa Allah tu; na nini kitakujulisha laala saa ile iko karibu.

يَسْـَٔلُكَ النَّاسُ عَنِ السَّاعَةِ ۭ قُلْ اِنَّمَا عِلْمُهَا عِنْدَ اللّٰهِ ۭ وَمَا يُدْرِيْكَ لَعَلَّ السَّاعَةَ تَكُوْنُ قَرِيْبًا ﴿٦٤﴾

65. Kwa hakika Allah Amewalaani makafiri na Amewaandalia Moto uwakao.

اِنَّ اللّٰهَ لَعَنَ الْكٰفِرِيْنَ وَاَعَدَّ لَهُمْ سَعِيْرًا ﴿٦٥﴾

66. Watakaa humo muda mrefu, hawatapata mlinzi wala msaidizi.

خٰلِدِيْنَ فِيْهَآ اَبَدًا ۚ لَا يَجِدُوْنَ وَلِيًّا وَّلَا نَصِيْرًا ﴿٦٦﴾

67. Siku ambayo nyuso zao zitapinduliwa Motoni, watasema: Laiti tungemtii Allah na tungemtii Mtume.

يَوْمَ تُقَلَّبُ وُجُوْهُهُمْ فِي النَّارِ يَقُوْلُوْنَ يٰلَيْتَنَآ اَطَعْنَا اللّٰهَ وَاَطَعْنَا الرَّسُوْلَا ﴿٦٧﴾

Maovu mengi ya ufasiki yanayoleta uadui baina ya watu, na kuwaondolea starehe na utulivu wa moyo, yanatokana na kupuuzwa amri hizi. Amri hizi zimekusudiwa kuing'oa kabisa mizizi ya maovu haya. Watu wataendelea kuwa katika mashaka maadamu hawatii amri hizi za Allah. Waislamu wanatakiwa kufanya kila juhudi - wake kwa waume - kuona ya kwamba maagizo haya ya Mwenyezi Mungu yanafuatwa kwa uaminifu. Kushikilia mambo ya ada na desturi za watu hakujapata kuleta heri duniani inapokuwa ada hizo zinapingana na hukumu za Allah. Mwanadamu hana busara pasipo kuongozwa na Allah. Desturi ya kuchanganyika ovyo wanawake na wanaume wasio na mipaka ya kuoana, na kuachwa maagizo yanayoelezwa na Aya hizi, ndiyo mambo yanayoimarisha maovu ya aina hii duniani, nayo ni moto unaounguza nyoyo na kuziteketeza, na kumfikisha mtu katika Moto mbaya zaidi siku ya Kiyama.

وَقَالُوْا رَبَّنَآ اِنَّآ اَطَعْنَا سَادَتَنَا وَكُبَرَآءَنَا فَاَضَلُّوْنَا السَّبِيْلَا ﴿٦٨﴾

68. Na watasema: Mola wetu, hakika tumewafuata mabwana wetu na wakubwa wetu, basi wao wametupoteza njia.

رَبَّنَآ اٰتِهِمْ ضِعْفَيْنِ مِنَ الْعَذَابِ وَالْعَنْهُمْ لَعْنًا كَبِيْرًا ﴿٦٩﴾ ع

69. Mola wetu: Uwape hawa adhabu maradufu na Uwalaani laana kubwa.

FUNGU 9

يٰٓاَيُّهَا الَّذِيْنَ اٰمَنُوْا لَا تَكُوْنُوْا كَالَّذِيْنَ اٰذَوْا مُوْسٰى فَبَرَّاَهُ اللّٰهُ مِمَّا قَالُوْا ؕ وَكَانَ عِنْدَ اللّٰهِ وَجِيْهًا ﴿٧٠﴾

70. Enyi mlioamini! msiwe kama wale waliomtaabisha Musa; basi Allah Akamtakasa na yale waliyoyasema, naye alikuwa mwenye heshima mbele ya Allah.

يٰٓاَيُّهَا الَّذِيْنَ اٰمَنُوا اتَّقُوا اللّٰهَ وَقُوْلُوْا قَوْلًا سَدِيْدًا ﴿٧١﴾

71. Enyi mlioamini, MwogopeniAllah na semeni usemi ulionyooka.

يُّصْلِحْ لَكُمْ اَعْمَالَكُمْ وَيَغْفِرْ لَكُمْ ذُنُوْبَكُمْ ؕ وَمَنْ يُّطِعِ اللّٰهَ وَرَسُوْلَهٗ فَقَدْ فَازَ فَوْزًا عَظِيْمًا ﴿٧٢﴾

72. Atawatengenezeeni vizuri vitendo vyenu na Atawasameheni madhambi yenu; na anayemtii Allah na Mtume Wake, bila shaka amefanikiwa mafanikio makubwa.

اِنَّا عَرَضْنَا الْاَمَانَةَ عَلَى السَّمٰوٰتِ وَالْاَرْضِ وَالْجِبَالِ فَاَبَيْنَ اَنْ يَّحْمِلْنَهَا وَاَشْفَقْنَ مِنْهَا وَحَمَلَهَا الْاِنْسَانُ ؕ اِنَّهٗ كَانَ ظَلُوْمًا جَهُوْلًا ﴿٧٣﴾

73. Kwa yakini Sisi Tulizitolea amana mbingu na ardhi na milima, lakini vikakataa kuichukua na vikaiogopa, lakini mwanadamu aliyekamilika akaichukua. Bila shaka yeye alikuwa ni mwenye kujidhulumu sana (nafsi yake) na asiyejali kabisa (matokeo ya jukumu hilo).

لِّيُعَذِّبَ اللّٰهُ الْمُنٰفِقِيْنَ وَالْمُنٰفِقٰتِ وَالْمُشْرِكِيْنَ وَالْمُشْرِكٰتِ وَيَتُوْبَ اللّٰهُ عَلَى الْمُؤْمِنِيْنَ وَالْمُؤْمِنٰتِ ؕ وَكَانَ اللّٰهُ غَفُوْرًا رَّحِيْمًا ﴿٧٤﴾ ع

74. Ili Allah Awaadhibu wanaume wanafiki na wanawake wanafiki, na wanaume washirikina na wanawake washirikina na Allah Awaelekee kwa rehema waaminio wanaume na waaminio wanawake; na Allah ni Msamehevu, Mrehemevu.

Aya 73. Mwanadamu tu ndiye anayekubali kujidhulumu kwa ajili ya huba ya Allah, na anaweza kuwa mjinga na akasahau mambo mengine yote kwa sababu ya mapenzi na Allah. Kwa hakika mwanadamu ndiye anayeweza kuchukua amana hii ya kudhihirisha sifa za Allah. Viumbe vingine haviwezi.

سُوْرَةُ سَبَإٍ مَّكِّيَّةٌ وَّ هِيَ مَعَ الْبَسْمَلَةِ خَمْسٌ وَّ خَمْسُوْنَ اٰيَةً وَّ سِتَّةُ رُكُوْعَاتٍ

34. SURA SABAA

Imeteremshwa Makka

Ina mafungu 6 na Aya 55 pamoja na Bismillahi

بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ ①

1. Kwa jina la Allah, Mwingi wa rehema, Mwingi wa ukarimu.

اَلْحَمْدُ لِلّٰهِ الَّذِيْ لَهٗ مَا فِي السَّمٰوٰتِ وَمَا فِي الْاَرْضِ وَ لَهُ الْحَمْدُ فِي الْاٰخِرَةِ ؕ وَهُوَ الْحَكِيْمُ الْخَبِيْرُ ②

2. Sifa zote njema ni za Allah Ambaye ni Vyake vilivyomo mbinguni na ardhini, na katika Akhera sifa njema ni Zake. Naye ni Mwenye hekima, Mwenye habari.

يَعْلَمُ مَا يَلِجُ فِي الْاَرْضِ وَمَا يَخْرُجُ مِنْهَا وَمَا يَنْزِلُ مِنَ السَّمَآءِ وَمَا يَعْرُجُ فِيْهَا ؕ وَهُوَ الرَّحِيْمُ الْغَفُوْرُ ③

3. Anajua yaingiayo ardhini na yatokayo humo na yateremkayo kutoka mbinguni na yapandayo humo; naye ni Mrehemevu, Msamehevu.

وَقَالَ الَّذِيْنَ كَفَرُوْا لَا تَاْتِيْنَا السَّاعَةُ ؕ قُلْ بَلٰى وَ رَبِّيْ لَتَاْتِيَنَّكُمْ ۙ عٰلِمِ الْغَيْبِ ۚ لَا يَعْزُبُ عَنْهُ مِثْقَالُ ذَرَّةٍ فِي السَّمٰوٰتِ وَلَا فِي الْاَرْضِ وَلَاۤ اَصْغَرُ مِنْ ذٰلِكَ وَلَاۤ اَكْبَرُ اِلَّا فِيْ كِتٰبٍ مُّبِيْنٍ ۙ ④

4. Na walisema waliokufuru: Haitatufikia saa ile. Sema: Naam, kwa haki ya Mola wangu, bila shaka (saa ile) itawafikieni - Ajuaye mambo ya siri, hakifichiki Kwake kitu cho chote kilicho na uzito wa chembe katika mbingu wala katika ardhi; wala kidogo kuliko hicho wala kikubwa zaidi ila vimo katika Kitabu kibainishacho.

لِّيَجْزِيَ الَّذِيْنَ اٰمَنُوْا وَعَمِلُوا الصّٰلِحٰتِ ؕ اُولٰٓئِكَ لَهُمْ مَّغْفِرَةٌ وَّ رِزْقٌ كَرِيْمٌ ⑤

5. Ili awalipe wale walioamini na kufanya vitendo vizuri; hao watalipwa msamaha na riziki yenye heshima.

وَالَّذِيْنَ سَعَوْ فِيْۤ اٰيٰتِنَا مُعٰجِزِيْنَ اُولٰٓئِكَ لَهُمْ عَذَابٌ مِّنْ رِّجْزٍ اَلِيْمٌ ⑥

6. Na wale wanaojitahidi kwenda huku na huko kutudhoofisha kuhusiana na ishara zetu hao wamekadiriwa adhabu iumizayo miongoni mwa adhabu zenye kutetemesha.

وَيَرَى الَّذِيْنَ اُوْتُوا الْعِلْمَ الَّذِيْۤ اُنْزِلَ اِلَيْكَ مِنْ رَّبِّكَ هُوَ الْحَقَّ ۙ وَ يَهْدِيْۤ اِلٰى صِرَاطِ الْعَزِيْزِ الْحَمِيْدِ ⑦

7. Na waliopewa elimu hufahamu ya kuwa yale yaliyoteremshwa kwako kutoka kwa Mola wako ndiyo haki, nayo huongoza kwenye njia ya Mwenye nguvu, Asifiwaye.

Sura hii imepewa jina la mji *Saba'* ambao ulikuwa katika nchi ya Yaman na ukagharikishwa kwa mafuriko ya mji. Sura hii ilishuka Makka.

وَقَالَ الَّذِيْنَ كَفَرُوْا هَلْ نَدُلُّكُمْ عَلٰى رَجُلٍ يُّنَبِّئُكُمْ اِذَا مُزِّقْتُمْ كُلَّ مُمَزَّقٍ ۙ اِنَّكُمْ لَفِيْ خَلْقٍ جَدِيْدٍ ۞٧

8. Na waliokufuru husema: Je, tuwajulisheni mtu anayewaambieni ya kwamba mtakapochambuliwa vipande-vipande hakika ninyi mtakuwa katika umbo jipya.

اَفْتَرٰى عَلَى اللّٰهِ كَذِبًا اَمْ بِهٖ جِنَّةٌ ؕ بَلِ الَّذِيْنَ لَا يُؤْمِنُوْنَ بِالْاٰخِرَةِ فِي الْعَذَابِ وَالضَّلٰلِ الْبَعِيْدِ ۞٨

9. Je, amezua uwongo juu ya Allah au amepata wazimu? Bali wasioamini Akhera watakuwa katika adhabu na upotevu wa mbali.

اَفَلَمْ يَرَوْا اِلٰى مَا بَيْنَ اَيْدِيْهِمْ وَمَا خَلْفَهُمْ مِّنَ السَّمَآءِ وَالْاَرْضِ ؕ اِنْ نَّشَاْ نَخْسِفْ بِهِمُ الْاَرْضَ اَوْ نُسْقِطْ عَلَيْهِمْ كِسَفًا مِّنَ السَّمَآءِ ؕ اِنَّ فِيْ ذٰلِكَ لَاٰيَةً لِّكُلِّ عَبْدٍ مُّنِيْبٍ ۞٩

10. Je, hawaoni yaliyo mbele yao na yaliyo nyuma yao ya mbingu na ya ardhi? Kama Tungependa Tungewadidimiza ardhini au Tungeangusha juu yao vipande vya mbingu. Bila shaka katika hayo iko Ishara kwa kila mtumishi mwelekevu.

FUNGU 2

وَلَقَدْ اٰتَيْنَا دَاوٗدَ مِنَّا فَضْلًا ؕ يٰجِبَالُ اَوِّبِيْ مَعَهٗ وَالطَّيْرَ ۚ وَاَلَنَّا لَهُ الْحَدِيْدَ ۞١٠

11. Na kwa hakika Tulimpa Daudi fadhili kutoka Kwetu, enyi milima nyenyekeeni pamoja naye, na ndege (pia); na Tukamlainishia chuma,

اَنِ اعْمَلْ سٰبِغٰتٍ وَّقَدِّرْ فِي السَّرْدِ وَاعْمَلُوْا صَالِحًا ؕ اِنِّيْ بِمَا تَعْمَلُوْنَ بَصِيْرٌ ۞١١

12. (Tukamwambia) ya kwamba tengeneza (deraya) pana na upime katika kuunganisha; na fanyeni vitendo vizuri; bila shaka Nayaona mnayoyatenda.

وَلِسُلَيْمٰنَ الرِّيْحَ غُدُوُّهَا شَهْرٌ وَّرَوَاحُهَا شَهْرٌ ۚ وَاَسَلْنَا لَهٗ عَيْنَ

13. Na kwa Suleimani (Tukautiisha) upepo (uliokwenda) safari yake ya asubuhi (mwendo wa) mwezi mmoja na safari yake ya jioni (mwendo wa) mwezi

Aya 11. *Tukamlainishia chuma*. Nabii Daudi alifundishwa na Allah namna ya kuyeyusha chuma na kukitumia kwa kazi mbalimbali.

Aya 13. *Riih,* "Upepo." Neno hili pengine mradi wake ni utawala na mamlaka yaliyoenea umbali wa mwendo wa mwezi mmoja magharibi na mashariki. Pia mradi wake inaweza kuwa merikebu za Nabii Suleimani ziliweza kwenda safari ya mwezi mmoja kwa siku moja kwa ajili ya pepo nzuri.

الْقِطْرِ ؕ وَمِنَ الْجِنِّ مَنْ يَّعْمَلُ بَيْنَ يَدَيْهِ بِاِذْنِ رَبِّهٖ ؕ وَمَنْ يَّزِغْ مِنْهُمْ عَنْ اَمْرِنَا نُذِقْهُ مِنْ عَذَابِ السَّعِيْرِ ﴿١٣﴾

mmoja; na Tukamtiririshia chemchem ya shaba. Na katika majinni (kulikuwa na) waliofanya kazi mbele yake kwa idhini ya Mola wake; na kila anayejitenga na amri Yetu miongoni mwao Tunamwonjesha adhabu ya Moto uwakao.

يَعْمَلُوْنَ لَهٗ مَا يَشَآءُ مِنْ مَّحَارِيْبَ وَتَمَاثِيْلَ وَجِفَانٍ كَالْجَوَابِ وَقُدُوْرٍ رّٰسِيٰتٍ ؕ اِعْمَلُوْٓا اٰلَ دَاوٗدَ شُكْرًا ؕ وَقَلِيْلٌ مِّنْ عِبَادِيَ الشَّكُوْرُ ﴿١٤﴾

14. Walikuwa wakimfanyia alipendalo, kama ngome na masanamu na sinia kubwa kama hodhi, na masufuria makubwa sana yasiyoondolewa kutoka mahali pao. Fanyeni kazi, enyi wana wa Daudi kwa kushukuru; na ni wachache wanaoshukuru katika watumishi Wangu.

فَلَمَّا قَضَيْنَا عَلَيْهِ الْمَوْتَ مَا دَلَّهُمْ عَلٰى مَوْتِهٖٓ اِلَّا دَآبَّةُ الْاَرْضِ تَاْكُلُ مِنْسَاَتَهٗ ۚ فَلَمَّا خَرَّ تَبَيَّنَتِ الْجِنُّ اَنْ لَّوْ كَانُوْا يَعْلَمُوْنَ الْغَيْبَ مَا لَبِثُوْا فِي الْعَذَابِ الْمُهِيْنِ ﴿١٥﴾

15. Na Tulipomkidhia (Suleiman) mauti hakuna kilichowabainishia kwamba yeye amekwisha kufa isipokuwa mdudu wa ardhini (mwanawe mwovu) aliyekuwa akiila fimbo (ya utawala) wake. Basi alipoanguka (ulipoangamia utawala wake) ndipo wale majini (watu wa milimani) wakatambua kwamba kama wangalikua na elimu ya ghaibu, wasingalibakia ndani ya adhabu hiyo ifedheheshayo.

لَقَدْ كَانَ لِسَبَاٍ فِيْ مَسْكَنِهِمْ اٰيَةٌ ۚ جَنَّتٰنِ عَنْ يَّمِيْنٍ وَّشِمَالٍ ؕ كُلُوْا مِنْ رِّزْقِ رَبِّكُمْ وَاشْكُرُوْا لَهٗ ؕ بَلْدَةٌ طَيِّبَةٌ وَّرَبٌّ غَفُوْرٌ ﴿١٦﴾

16. Bila shaka ilikuwa Ishara kwa Saba' katika maskani yao. Bustani mbili kulia na kushoto. Kuleni katika riziki ya Mola wenu, na mumshukuru: mji mzuri na Mola Msamehevu.

Aya 14. *Aala Daawuuda* "Wana wa Daudi," pia maana yake ni wafuasi wa Daudi.

Aya 15. Neno *daabbah* linatumika kuhusiana na aina zote za wanyama. Kwa hiyo tafsiri "mdudu wa ardhini" yapasa ichukuliwe kimethali na wala si kwa maana ya neno kwa neno. Rejea hii inamhusu mwana wa Suleimani ambaye hakurithi chochote miongoni mwa sifa za kiroho wala ustadi wa kutawala zilizompambanua Suleimani, baba yake aliyekuwa mashuhuri. Wakati wa utawala wake iliwabainikia pole pole wale machifu wenye nguvu (majini), ambao walikuwa wamezidiwa nguvu na kutiishwa na Suleimani, kwamba Suleimani sasa alikuwa amekufa kikweli kweli. Wakafanikiwa kuiasi serikali na wakasababisha ile dola kubwa ivunjike vipande vipande.

Aya 16. *Sabaa* lilikuwa jina la mtu mmoja ambaye alikuwa na watoto kumi. Ulijengwa mji ukapewa jina lake. Mahali hapo palikuwa na mwendo wa siku tatu kutoka Sanaa huko Yemen.

فَاَعۡرَضُوۡا فَاَرۡسَلۡنَا عَلَيۡهِمۡ سَيۡلَ الۡعَرِمِ
وَبَدَّلۡنٰهُمۡ بِجَنَّتَيۡهِمۡ جَنَّتَيۡنِ ذَوَاتَىۡ اُكُلٍ
خَمۡطٍ وَّاَثۡلٍ وَّشَىۡءٍ مِّنۡ سِدۡرٍ قَلِيۡلٍ ﴿١٧﴾

17. Lakini wakajitenga; kwa hiyo Tukawapelekea furiko kubwa na Tukawabadilishia bustani zao kwa bustani nyingine mbili zenye matunda yaliyochachuka na vichaka na miti michache ya mikunazi.

ذٰلِكَ جَزَيۡنٰهُمۡ بِمَا كَفَرُوۡا ؕ وَهَلۡ نُجٰزِىۡۤ
اِلَّا الۡكَفُوۡرَ ﴿١٨﴾

18. Haya Tuliwalipa kwa sababu walikufuru. Nasi Hatumwadhibu ila asiye na shukrani.

وَجَعَلۡنَا بَيۡنَهُمۡ وَبَيۡنَ الۡقُرَى الَّتِىۡ بٰرَكۡنَا
فِيۡهَا قُرًى ظَاهِرَةً وَّقَدَّرۡنَا فِيۡهَا السَّيۡرَ ؕ
سِيۡرُوۡا فِيۡهَا لَيَالِىَ وَاَيَّامًا اٰمِنِيۡنَ ﴿١٩﴾

19. Na baina yao na baina ya miji Tuliyoibariki, Tukaweka miji iliyo dhahiri, na Tukapima humo(kambi za) safari. Tembeeni humo usiku na mchana kwa amani.

فَقَالُوۡا رَبَّنَا بٰعِدۡ بَيۡنَ اَسۡفَارِنَا وَظَلَمُوۡۤا
اَنۡفُسَهُمۡ فَجَعَلۡنٰهُمۡ اَحَادِيۡثَ وَمَزَّقۡنٰهُمۡ
كُلَّ مُمَزَّقٍ ؕ اِنَّ فِىۡ ذٰلِكَ لَاٰيٰتٍ لِّكُلِّ صَبَّارٍ
شَكُوۡرٍ ﴿٢٠﴾

20. Basi wakasema: Mola wetu, Uweke mwendo mrefu baina ya safari zetu; na wakajidhulumu nafsi zao. Ndipo Tukawafanya hadithi na Tukawararua vipande-vipande; kwa hakika katika hayo zimo Ishara kwa kila afanyaye subira sana, mwenye shukrani.

وَلَقَدۡ صَدَّقَ عَلَيۡهِمۡ اِبۡلِيۡسُ ظَنَّهٗ
فَاتَّبَعُوۡهُ اِلَّا فَرِيۡقًا مِّنَ الۡمُؤۡمِنِيۡنَ ﴿٢١﴾

21. Na bila shaka Ibilisi alisadikisha dhana yake juu yao, nao wakamfuata isipokuwa kundi la waaminio.

وَمَا كَانَ لَهٗ عَلَيۡهِمۡ مِّنۡ سُلۡطٰنٍ اِلَّا لِنَعۡلَمَ
مَنۡ يُّؤۡمِنُ بِالۡاٰخِرَةِ مِمَّنۡ هُوَ مِنۡهَا فِىۡ
شَكٍّ ؕ وَرَبُّكَ عَلٰى كُلِّ شَىۡءٍ حَفِيۡظٌ ﴿٢٢﴾ ع ٨

22. Na yeye hakuwa na mamlaka yo yote juu yao, ila kwa sababu Tudhihirishe ni nani mwenye kuamini Akhera na nani aioneaye shaka; na Mola wako ni Mhifadhi wa kila kitu.

FUNGU 3

قُلِ ادۡعُوا الَّذِيۡنَ زَعَمۡتُمۡ مِّنۡ دُوۡنِ اللّٰهِ ۚ
لَا يَمۡلِكُوۡنَ مِثۡقَالَ ذَرَّةٍ فِى السَّمٰوٰتِ وَلَا
فِى الۡاَرۡضِ وَمَا لَهُمۡ فِيۡهِمَا مِنۡ شِرۡكٍ
وَّمَا لَهٗ مِنۡهُمۡ مِّنۡ ظَهِيۡرٍ ﴿٢٢﴾

23. Sema: Waiteni mnaowadai kinyume cha Allah; wao hawamiliki uzito wa chembe mbinguni wala ardhini, wala hawana ushirika katika hizo; wala Yeye Hana msaidizi miongoni mwao.

Aya 18. *Wanaokufuru,* hapa mradi wake ni wasioshukuru.

وَلَا تَنْفَعُ الشَّفَاعَةُ عِنْدَهٗٓ اِلَّا لِمَنْ اَذِنَ لَهٗ ؕ حَتّٰٓى اِذَا فُزِّعَ عَنْ قُلُوْبِهِمْ قَالُوْا مَاذَا ۙ قَالَ رَبُّكُمْ ؕ قَالُوا الْحَقَّ ۚ وَهُوَ الْعَلِيُّ الْكَبِيْرُ ﴿٢٣﴾

24. Wala hautafaa uombezi mbele Yake ila kwa yule Aliyempa idhini. Hata inapoondolewa hofu mioyoni mwao, wanasema: Mola wenu Amesema nini? Wanasema: Haki, naye ndiye Aliye juu Mkubwa.

قُلْ مَنْ يَّرْزُقُكُمْ مِّنَ السَّمٰوٰتِ وَالْاَرْضِ ؕ قُلِ اللّٰهُ ۙ وَاِنَّآ اَوْ اِيَّاكُمْ لَعَلٰى هُدًى اَوْ فِيْ ضَلٰلٍ مُّبِيْنٍ ﴿٢٤﴾

25. Sema: Ni nani anayewaruzukuni kutoka mbinguni na ardhini? Sema: Allah; na bila shaka ni sisi au ninyi tulio juu ya mwongozo au katika upotevu ulio wazi.

قُلْ لَّا تُسْـَٔلُوْنَ عَمَّآ اَجْرَمْنَا وَلَا نُسْـَٔلُ عَمَّا تَعْمَلُوْنَ ﴿٢٥﴾

26. Sema: Hamtaulizwa kwa makosa tuliyoyafanya, wala hatutaulizwa kwa yale mnayoyatenda.

قُلْ يَجْمَعُ بَيْنَنَا رَبُّنَا ثُمَّ يَفْتَحُ بَيْنَنَا بِالْحَقِّ ؕ وَهُوَ الْفَتَّاحُ الْعَلِيْمُ ﴿٢٦﴾

27. Sema: Mola wetu Atatukusanya baina yetu kisha Atahukumu baina yetu kwa haki; naye ndiye Hakimu, Ajuaye.

قُلْ اَرُوْنِيَ الَّذِيْنَ اَلْحَقْتُمْ بِهٖ شُرَكَآءَ كَلَّا ؕ بَلْ هُوَ اللّٰهُ الْعَزِيْزُ الْحَكِيْمُ ﴿٢٧﴾

28. Sema: Nionyesheni wale mliowaunganisha naye kuwa washirika; haiwezekani. Lakini Yeye ndiye Allah, Mwenye ushindi kamili, Mwenye hekima.

وَمَآ اَرْسَلْنٰكَ اِلَّا كَآفَّةً لِّلنَّاسِ بَشِيْرًا وَّنَذِيْرًا وَّلٰكِنَّ اَكْثَرَ النَّاسِ لَا يَعْلَمُوْنَ ﴿٢٨﴾

29. Na Hatukukutuma ila kwa watu wote uwe Mtoaji wa habari njema na Mwonyaji; lakini watu wengi hawajui.

وَيَقُوْلُوْنَ مَتٰى هٰذَا الْوَعْدُ اِنْ كُنْتُمْ صٰدِقِيْنَ ﴿٢٩﴾

30. Na wanasema: Lini (itatimia) ahadi hii ikiwa mnasema kweli?

قُلْ لَّكُمْ مِّيْعَادُ يَوْمٍ لَّا تَسْتَاْخِرُوْنَ عَنْهُ سَاعَةً وَّلَا تَسْتَقْدِمُوْنَ ﴿٣٠﴾ ع

31. Sema: Mmepewa miadi ya siku ambayo hamtaiahirisha saa wala hamtaitanguliza.

Aya 27. *Atatukusanya baina yetu,* yaani katika vita.

Aya 29. Aya hii inaeleza waziwazi kuwa Mtume *s.a.w.* ametumwa kwa watu wote wa dunia.

Aya 30. Inaonyesha makafiri walifahamu mkusanyo huu ni wa jambo gani, na wakauliza utakuwa lini.

Aya 31. Hapa inatolewa ahadi ya *siku moja.* Katika bishara siku moja ni sawa na mwaka mmoja. Basi alipohama Mtume *s.a.w.* kwenda Madina, ulipopita mwaka , makafiri walileta vita

FUNGU 4

وَقَالَ الَّذِيْنَ كَفَرُوْا لَنْ نُّؤْمِنَ بِهٰذَا الْقُرْاٰنِ وَلَا بِالَّذِيْ بَيْنَ يَدَيْهِ ؕ وَلَوْ تَرٰٓى اِذِ الظّٰلِمُوْنَ مَوْقُوْفُوْنَ عِنْدَ رَبِّهِمْ ۖۚ يَرْجِعُ بَعْضُهُمْ اِلٰى بَعْضِ ِۨالْقَوْلَ ۚ يَقُوْلُ الَّذِيْنَ اسْتُضْعِفُوْا لِلَّذِيْنَ اسْتَكْبَرُوْا لَوْلَآ اَنْتُمْ لَكُنَّا مُؤْمِنِيْنَ ۝٣١

32. Na wakasema wale waliokufuru: Hatutaiamini kabisa Qur'an hii , wala (bishara) zile zilizoko mbele yake: na laiti ungewaona wadhalimu watakaposimamishwa mbele ya Mola wao, wakirudishiana maneno wao kwa wao! Wale waliofahamiwa kuwa wanyonge watawaambia wale waliojiona wakubwa: Kama si ninyi bila shaka tungekuwa waaminio.

قَالَ الَّذِيْنَ اسْتَكْبَرُوْا لِلَّذِيْنَ اسْتُضْعِفُوْٓا اَنَحْنُ صَدَدْنٰكُمْ عَنِ الْهُدٰى بَعْدَ اِذْ جَآءَكُمْ بَلْ كُنْتُمْ مُّجْرِمِيْنَ ۝٣٢

33. Watasema wale waliojiona wakubwa kuwaambia wale waliofahamiwa kuwa wanyonge: Je, sisi tuliwakatazeni mwongozo baada ya kuwafikieni? Bali ninyi wenyewe mlikuwa wakosefu.

وَقَالَ الَّذِيْنَ اسْتُضْعِفُوْا لِلَّذِيْنَ اسْتَكْبَرُوْا بَلْ مَكْرُ الَّيْلِ وَالنَّهَارِ اِذْ تَاْمُرُوْنَنَآ اَنْ نَّكْفُرَ بِاللّٰهِ وَنَجْعَلَ لَهٗٓ اَنْدَادًا ؕ وَاَسَرُّوا النَّدَامَةَ لَمَّا رَاَوُا الْعَذَابَ ؕ وَجَعَلْنَا الْاَغْلٰلَ فِيْٓ اَعْنَاقِ الَّذِيْنَ كَفَرُوْا ؕ هَلْ يُجْزَوْنَ اِلَّا مَا كَانُوْا يَعْمَلُوْنَ ۝٣٣

34. Na wale waliofahamiwa wanyonge watasema kuwaambia wale waliojiona wakubwa: Bali (mlikuwa mkifanya) hila usiku na mchana mlipotuamuru tumkufuru Allah na tumfanyie washirika. Nao wataficha majuto watakapoiona adhabu; na Tutaweka minyororo mashingoni mwa wale waliokufuru; hawatalipwa ila yale yale waliyokuwa wakiyatenda.

---

iliyopiganwa Badri na wakashindwa; na kwa njia hii hukumu ya Allah ikatolewa kuonyesha upande gani una haki.

Bishara hii pia imeelezwa katika kitabu cha Isaya 21:16 ya kuwa katika mwaka mmoja heshima ya Waarabu (Kedar) itavunjika kwa sababu ya kushindana na haki.

Aya 32. *Wala yale yaliyokuwa kabla yake.* Walikataa hata vitabu vya zamani kwa sababu navyo vilikuwa na Ishara za kufika kwa Mtume *s.a.w.* Mtu anaposhikwa na uwadui haoni haki wala Ishara.

Aya 34. *Wataficha majuto.* Maneno ya Kiarabu yaliyofasiriwa hivyo pia yana maana ya "watadhihirisha majuto."

وَمَآ اَرْسَلْنَا فِيْ قَرْيَةٍ مِّنْ نَّذِيْرٍ اِلَّا قَالَ مُتْرَفُوْهَآ ۙ اِنَّا بِمَآ اُرْسِلْتُمْ بِهٖ كٰفِرُوْنَ ﴿٣٥﴾

35. Na Hatukumtuma Mwonyaji katika mji wo wote ila matajiri wa mji ule walisema, "Kwa yakini sisi tunayakataa hayo mliyotumwa kuyaleta."

وَقَالُوْا نَحْنُ اَكْثَرُ اَمْوَالًا وَّاَوْلَادًا ۙ وَّمَا نَحْنُ بِمُعَذَّبِيْنَ ﴿٣٦﴾

36. Na wakasema: Sisi tunazo mali nyingi na watoto wengi, wala sisi hatutaadhibiwa.

قُلْ اِنَّ رَبِّيْ يَبْسُطُ الرِّزْقَ لِمَنْ يَّشَآءُ وَيَقْدِرُ وَلٰكِنَّ اَكْثَرَ النَّاسِ لَا يَعْلَمُوْنَ ﴿٣٧﴾ ع

37. Sema: Kwa yakini Mola wangu Humfungulia riziki Amtakaye na Humdhikisha; lakini watu wengi hawajui.

FUNGU 5

وَمَآ اَمْوَالُكُمْ وَلَآ اَوْلَادُكُمْ بِالَّتِيْ تُقَرِّبُكُمْ عِنْدَنَا زُلْفٰٓى اِلَّا مَنْ اٰمَنَ وَعَمِلَ صَالِحًا ۚ فَاُولٰٓئِكَ لَهُمْ جَزَآءُ الضِّعْفِ بِمَا عَمِلُوْا وَهُمْ فِي الْغُرُفٰتِ اٰمِنُوْنَ ﴿٣٨﴾

38. Na si mali zenu wala watoto wenu watakaowafanyeni muwe karibu nasi katika daraja, isipokuwa aliyeamini na kutenda mema. Basi hao watapata ujira mara mbili kwa yale waliyotenda, nao watakuwa salama katika maghorofa.

وَالَّذِيْنَ يَسْعَوْنَ فِيْٓ اٰيٰتِنَا مُعٰجِزِيْنَ اُولٰٓئِكَ فِي الْعَذَابِ مُحْضَرُوْنَ ﴿٣٩﴾

39. Na wale wanaojitahidi kuzipinga Aya Zetu, hao watahudhurishwa adhabuni.

قُلْ اِنَّ رَبِّيْ يَبْسُطُ الرِّزْقَ لِمَنْ يَّشَآءُ مِنْ عِبَادِهٖ وَيَقْدِرُ لَهٗ ۭ وَمَآ اَنْفَقْتُمْ مِّنْ شَيْءٍ فَهُوَ يُخْلِفُهٗ ۚ وَهُوَ خَيْرُ الرّٰزِقِيْنَ ﴿٤٠﴾

40. Sema: Kwa hakika Mola wangu Humkunjulia riziki Amtakaye katika watumishi Wake, na Humdhikishia. Na cho chote mtakachotoa, basi ni Yeye Atakayekilipa; naye ni Mbora wa wanaoruzuku.

وَيَوْمَ يَحْشُرُهُمْ جَمِيْعًا ثُمَّ يَقُوْلُ لِلْمَلٰٓئِكَةِ اَهٰٓؤُلَآءِ اِيَّاكُمْ كَانُوْا يَعْبُدُوْنَ ﴿٤١﴾

41. Na siku Atakapowakusanya wote kisha Atawaambia Malaika: Je hawa ndio walikuwa wakiwaabuduni?

Aya 40. *Atakayekilipa*. Masahaba walitoa vitu vyao katika njia ya Allah, naye akawalipa milki kubwa hapa hapa duniani. Hivyo anayetoa mali zake na wakati wake na nguvu zake katika njia ya Allah, hawezi kupata hasara, bali Allah atamzidishia malipo.

قَالُوْا سُبْحٰنَكَ اَنْتَ وَلِيُّنَا مِنْ دُوْنِهِمْ ۚ
بَلْ كَانُوْا يَعْبُدُوْنَ الْجِنَّ ۚ اَكْثَرُهُمْ
بِهِمْ مُّؤْمِنُوْنَ ﴿٤٢﴾

42. Watasema: Umeepukana na kila upungufu! Wewe ndiwe mlinzi wetu si hao; bali walikuwa wakiwaabudu majinni; wengi wao waliwaamini.

فَالْيَوْمَ لَا يَمْلِكُ بَعْضُكُمْ لِبَعْضٍ نَّفْعًا
وَّلَا ضَرًّا ؕ وَنَقُوْلُ لِلَّذِيْنَ ظَلَمُوْا ذُوْقُوْا
عَذَابَ النَّارِ الَّتِيْ كُنْتُمْ بِهَا تُكَذِّبُوْنَ ﴿٤٣﴾

43. Na hii leo hawataweza baadhi yenu kuwafaidia wengine, wala kuwadhuru; na Tutawaambia wale waliodhulumu: Onjeni adhabu ya Moto mliokuwa mkiukadhibisha.

وَاِذَا تُتْلٰى عَلَيْهِمْ اٰيٰتُنَا بَيِّنٰتٍ قَالُوْا مَا هٰذَاۤ
اِلَّا رَجُلٌ يُّرِيْدُ اَنْ يَّصُدَّكُمْ عَمَّا كَانَ
يَعْبُدُ اٰبَآؤُكُمْ ۚ وَقَالُوْا مَا هٰذَاۤ اِلَّاۤ
اِفْكٌ مُّفْتَرًى ؕ وَقَالَ الَّذِيْنَ كَفَرُوْا
لِلْحَقِّ لَمَّا جَآءَهُمْ ۙ اِنْ هٰذَاۤ اِلَّا سِحْرٌ
مُّبِيْنٌ ﴿٤٤﴾

44. Na wanaposomewa Aya Zetu zilizo wazi, husema: Huyu siye ila ni mtu anayetaka kuwazuieni katika yale waliyokuwa wakiabudu baba zenu. Wakasema: Siyo haya ila ni uwongo uliotungwa; na wakasema wale walioikataa haki ilipowafikia: Siyo haya ila ni uchawi ulio dhahiri.

وَمَاۤ اٰتَيْنٰهُمْ مِّنْ كُتُبٍ يَّدْرُسُوْنَهَا وَمَاۤ
اَرْسَلْنَاۤ اِلَيْهِمْ قَبْلَكَ مِنْ نَّذِيْرٍ ﴿٤٥﴾ؕ

45. Wala Hatukuwapa vitabu wanavyovisoma, wala hatukuwapelekea Mwonyaji kabla yako.

وَكَذَّبَ الَّذِيْنَ مِنْ قَبْلِهِمْ ۙ وَمَا بَلَغُوْا
مِعْشَارَ مَاۤ اٰتَيْنٰهُمْ فَكَذَّبُوْا رُسُلِيْ ۫
فَكَيْفَ كَانَ نَكِيْرِ ﴿٤٦﴾ ع

46. Na walikadhibisha wale waliokuwa kabla yao; na hawajafikia hata sehemu ya kumi ya Tulivyowapa hao; lakini waliwakadhibisha Mitume Wangu. Basi adhabu Yangu ilikuwa namna gani?

FUNGU 6

قُلْ اِنَّمَاۤ اَعِظُكُمْ بِوَاحِدَةٍ ۚ اَنْ تَقُوْمُوْا
لِلّٰهِ مَثْنٰى وَفُرَادٰى ثُمَّ تَتَفَكَّرُوْا ۫ مَا
بِصَاحِبِكُمْ مِّنْ جِنَّةٍ ؕ اِنْ هُوَ اِلَّا نَذِيْرٌ
لَّكُمْ بَيْنَ يَدَيْ عَذَابٍ شَدِيْدٍ ﴿٤٧﴾

47. Sema: Mimi nakunasihini kwa jambo moja tu ya kwamba msimame kwa ajili ya Allah, wawili-wawili na mmoja-mmoja, kisha mtafakari. Mwenzenu hana wazimu; yeye siye ila ni Mwonyaji wenu kabla ya kufika adhabu kali.

قُلْ مَا سَاَلْتُكُمْ مِّنْ اَجْرٍ فَهُوَ لَكُمْ ؕ اِنْ
اَجْرِيَ اِلَّا عَلَى اللّٰهِ ۚ وَهُوَ عَلٰى كُلِّ شَيْءٍ

48. Sema: Ujira wowote ninaowaombeni, basi huo ni kwa ajili yenu; ujira wangu uko

kwa Allah tu, naye ni Shahidi juu ya kila kitu.

49. Sema: Bila shaka Mola wangu Hutoa haki tu, Mjuzi wa (mambo ya) ghaibu.

50. Sema, Haki imeshafika na uwongo hauwezi kuanzilisha wala kurejesha cho chote.

51. Sema: Kama nikipotea, basi nitapotea kwa kuidhuru nafsi yangu tu; na kama nikiongoka, basi ni kwa sababu tu Ananifunulia Mola wangu. Bila shaka Yeye ni Asikiaye, Aliye karibu.

52. Na ungaliona watakapohangaika lakini hakuna kimbilio, na watakamatiwa mahali pa karibu.

53. Na watasema, "Sasa tunaiamini". Lakini wanawezaje kuishika imani kutokea mahali pa mbali?

54. Bila shaka walikwisha ikataa tangu zamani, wanakisia yasiyoonekana toka mahali pa mbali.

55. Na watatiliwa kizuizi kati yao na kati ya yale wanayoyatamani, kama walivyofanyiwa rafiki zao zamani; bila shaka walikuwa katika shaka ihangaishayo.

شَهِيْدٌ ﴿٤٨﴾

قُلْ اِنَّ رَبِّيْ يَقْذِفُ بِالْحَقِّ ۚ عَلَّامُ الْغُيُوْبِ ﴿٤٩﴾

قُلْ جَآءَ الْحَقُّ وَمَا يُبْدِئُ الْبَاطِلُ وَمَا يُعِيْدُ ﴿٥٠﴾

قُلْ اِنْ ضَلَلْتُ فَاِنَّمَآ اَضِلُّ عَلٰى نَفْسِيْ ۚ وَاِنِ اهْتَدَيْتُ فَبِمَا يُوْحِيْٓ اِلَيَّ رَبِّيْ ؕ اِنَّهٗ سَمِيْعٌ قَرِيْبٌ ﴿٥١﴾

وَلَوْ تَرٰٓى اِذْ فَزِعُوْا فَلَا فَوْتَ وَاُخِذُوْا مِنْ مَّكَانٍ قَرِيْبٍ ﴿٥٢﴾

وَّقَالُوْٓا اٰمَنَّا بِهٖ ۚ وَاَنّٰى لَهُمُ التَّنَاوُشُ مِنْ مَّكَانٍۢ بَعِيْدٍ ﴿٥٣﴾

وَّقَدْ كَفَرُوْا بِهٖ مِنْ قَبْلُ ۚ وَيَقْذِفُوْنَ بِالْغَيْبِ مِنْ مَّكَانٍۢ بَعِيْدٍ ﴿٥٤﴾

وَحِيْلَ بَيْنَهُمْ وَبَيْنَ مَا يَشْتَهُوْنَ كَمَا فُعِلَ بِاَشْيَاعِهِمْ مِّنْ قَبْلُ ؕ اِنَّهُمْ كَانُوْا فِيْ شَكٍّ مُّرِيْبٍ ﴿٥٥﴾ ع ١٣

Aya 52. Walikamatwa Badri na pia walikamatwa Makka.

Aya 53. Kwa kifupi ina maana tu kwamba kwa kuwa walikwisha kaa nayo mbali tangu mapema, hawawezi kuifikia imani baada ya kufika kwa adhabu.

Aya 54. Walikisia tu kuwa Mtume hatafanikiwa na hali hawana habari za ghaibu.

Aya 55. Adhabu kali ni mtu kukosa kupata kitu anachotamani mno. Na makafiri watazuiliwa kupata wanayoyatamani.

سُوْرَةُ فَاطِرٍ مَّكِّيَّةٌ وَّ هِيَ مَعَ الْبَسْمَلَةِ سِتٌّ وَّ اَرْبَعُوْنَ اٰيَةً وَّ خَمْسَةُ رُكُوْعَاتٍ

35. SURA FAATIR

Imeteremshwa Makka

Ina mafungu 5 na Aya 46 pamoja na Bismillahi

بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ ①

اَلْحَمْدُ لِلّٰهِ فَاطِرِ السَّمٰوٰتِ وَالْاَرْضِ
جَاعِلِ الْمَلٰٓئِكَةِ رُسُلًا اُولِيْٓ اَجْنِحَةٍ
مَّثْنٰى وَثُلٰثَ وَرُبٰعَ ؕ يَزِيْدُ فِي الْخَلْقِ مَا
يَشَآءُ ؕ اِنَّ اللّٰهَ عَلٰى كُلِّ شَيْءٍ قَدِيْرٌ ②

1. Kwa jina la Allah, Mwingi wa rehema, Mwingi wa ukarimu.

2. Sifa zote njema ni za Allah, Mwumba wa mbingu na ardhi, Awafanyao Malaika kuwa wajumbe wenye mbawa mbili-mbili na tatu-tatu, na nne-nne. Huzidisha katika kuumba Apendavyo; bila shaka Allah ni Mwenye uwezo juu ya kila kitu.

Jina la sura hii limetoka katika sifa ya Allah iliyomo katika aya ya 2. Sura hii pia ilishuka Makka.

Aya 2. *Malaika.* Neno "Malaika" maana yake ni "mchukuzi wa ujumbe" au "wakili." Wao huleta ujumbe wa Allah na kupitisha Anayoyataka. Kama vile Allah ameweka taratibu katika ulimwengu wa kimwili, pia ameweka taratibu katika ulimwengu wa kiroho. Katika ulimwengu wa kimwili wao ni kiungo cha kwanza kwa kuungana na viungo vingine vinavyoshuka chini katika kuendesha kawaida za asili. Lakini katika ulimwengu wa kiroho wao ni kiungo cha moja kwa moja baina ya mtu na Allah.

Hatuwezi kufahamu kabisa umbo la Malaika, lakini tunaweza kufahamu kusudi la kuumbwa kwao na kazi wanazotakiwa kuzifanya. Dini ya Kiislamu inafundisha kuwa Malaika ni wengi kabisa na wamegawanywa katika sehemu mbalimbali, kila sehemu ina mahali maalumu na kusudi maalumu.

Islam inafundisha kuwaamini Malaika maana bila kuwaamini ni kama kuziba njia inayopita nuru ya Allah kuwaafikia watu.

Malaika hawaonekani kwa macho lakini baadhi ya wakati hujitokeza na wanaonekana kwa watu kwa sura mbalimbali. Siyo maana yake hizo ni sura zao hasa, bali huwa ni maonesho tu, wala siyo wameondoka mahali pao mbinguni.

Kuna hadithi nyingi zinazoeleza kuwa Malaika walijitokeza kwa Mtume *s.a.w.* kwa sura mbalimbali.

Kazi za Malaika zilizotajwa na Qur'an baadhi yao ni hizi:

(1) Wanaleta ujumbe wa Allah (sura 22:76). (2) Wanawatia watu mawazo ya kutenda mema na kuielekeza mioyo yao kwenye heri (sura 91:9 pia Tirmidh sura *Tafsir*). (3) Wanawatumikia Mitume na kuisaidia kazi yao (sura 15:30; 4:167); pia wanawasaidia waaminio (sura 41:31, 32). (4) Wanaleta adhabu kwa watu wanaowapinga Mitume (sura 6:159); na wanawatia hofu maadui zao (sura 3:125, 126). (5) Wanaziendesha kawaida za asili, na kama ilivyo wanakibeba Kiti cha Enzi cha Allah mabegani mwao (sura 40:8).

مَا يَفْتَحِ اللّٰهُ لِلنَّاسِ مِنْ رَّحْمَةٍ فَلَا
مُمْسِكَ لَهَا ۚ وَمَا يُمْسِكْ ۙ فَلَا مُرْسِلَ لَهٗ
مِنْۢ بَعْدِهٖ ؕ وَهُوَ الْعَزِيْزُ الْحَكِيْمُ ۝٢

3. Rehema Anayoifungua Allah kwa watu, hakuna wa kuizuia; na Aizuiayo hakuna wa kuipeleka isipokuwa Yeye, naye ni Mwenye ushindi kamili, Mwenye hekima.

يٰۤاَيُّهَا النَّاسُ اذْكُرُوْا نِعْمَتَ اللّٰهِ عَلَيْكُمْ ؕ
هَلْ مِنْ خَالِقٍ غَيْرُ اللّٰهِ يَرْزُقُكُمْ مِّنَ
السَّمَآءِ وَالْاَرْضِ ؕ لَاۤ اِلٰهَ اِلَّا هُوَ ۚ فَاَنّٰى
تُؤْفَكُوْنَ ۝٤

4. Enyi watu! Kumbukeni neema za Allah zilizoko juu yenu. Je, yuko mwumba mwingine ghairi ya Allah anayewapeni riziki kutoka mbinguni na ardhini? Hakuna aabudiwaye ila Yeye tu; basi wapi mnakopinduliwa?

وَاِنْ يُّكَذِّبُوْكَ فَقَدْ كُذِّبَتْ رُسُلٌ مِّنْ
قَبْلِكَ ؕ وَاِلَى اللّٰهِ تُرْجَعُ الْاُمُوْرُ ۝٥

5. Na kama wanakukadhibisha, basi wamekwisha kadhibishwa Mitume kabla yako; na mambo yote yatarudishwa kwa Allah.

يٰۤاَيُّهَا النَّاسُ اِنَّ وَعْدَ اللّٰهِ حَقٌّ فَلَا
تَغُرَّنَّكُمُ الْحَيٰوةُ الدُّنْيَا ۪ وَلَا يَغُرَّنَّكُمْ
بِاللّٰهِ الْغَرُوْرُ ۝٦

6. Enyi watu! bila shaka ahadi ya Allah ni haki, basi yasikudanganyeni maisha ya dunia, wala mdanganyaji asikudanganyeni juu ya Allah.

اِنَّ الشَّيْطٰنَ لَكُمْ عَدُوٌّ فَاتَّخِذُوْهُ عَدُوًّا ؕ
اِنَّمَا يَدْعُوْا حِزْبَهٗ لِيَكُوْنُوْا مِنْ اَصْحٰبِ
السَّعِيْرِ ؕ ۝٧

7. Kwa yakini Shetani ni adui yenu, basi mhesabuni kuwa adui: anawaita kundi lake tu ili wawe katika watu wa Moto uwakao.

اَلَّذِيْنَ كَفَرُوْا لَهُمْ عَذَابٌ شَدِيْدٌ ؕ
وَالَّذِيْنَ اٰمَنُوْا وَعَمِلُوا الصّٰلِحٰتِ لَهُمْ
مَّغْفِرَةٌ وَّاَجْرٌ كَبِيْرٌ ۝٨ ع ١٣

8. Waliokufuru itakuwa kwao adhabu kali, na wale walioamini na wakatenda mema, wao watapata msamaha na ujira mkubwa.

Mbawa mradi wake ni nguvu na uwezo. Malaika wamepewa nguvu mbalimbali sawa na kazi mbalimbali wanazozifanya. Wengine wana nguvu zaidi kuliko wengine.

Aya 6. *Gharuur.* Neno hili maana yake ni "mdanganyaji." Lakini kama likiwa *ghuruur* maana yake inakuwa "udanganyifu."

FUNGU 2

اَفَمَنْ زُيِّنَ لَهٗ سُوْٓءُ عَمَلِهٖ فَرَاٰهُ حَسَنًا ؕ فَاِنَّ اللّٰهَ يُضِلُّ مَنْ يَّشَآءُ وَيَهْدِيْ مَنْ يَّشَآءُ ۖ فَلَا تَذْهَبْ نَفْسُكَ عَلَيْهِمْ حَسَرٰتٍ ؕ اِنَّ اللّٰهَ عَلِيْمٌۢ بِمَا يَصْنَعُوْنَ ۝٨

9. Basi je, yule aliyepambiwa ubaya wa amali yake na akaiona kuwa njema (basi ni nani awezaye kudanganyika zaidi ya huyo?), Bila shaka Allah Humwacha kupotea Amtakaye na Humwongoza Amtakaye. Basi roho yako isitoke kwa majonzi juu yao; kwa yakini Allah Anayajua wanayoyafanya.

وَاللّٰهُ الَّذِيْٓ اَرْسَلَ الرِّيٰحَ فَتُثِيْرُ سَحَابًا فَسُقْنٰهُ اِلٰى بَلَدٍ مَّيِّتٍ فَاَحْيَيْنَا بِهِ الْاَرْضَ بَعْدَ مَوْتِهَا ؕ كَذٰلِكَ النُّشُوْرُ ۝٩

10. Na Allah ndiye Anayepeleka pepo zikainua mawingu na Tukayafikisha kwenye nchi iliyokufa, na kwayo Tukaihuisha ardhi baada ya kufa kwake; kama hivyo ndivyo ufufuo.

مَنْ كَانَ يُرِيْدُ الْعِزَّةَ فَلِلّٰهِ الْعِزَّةُ جَمِيْعًا ؕ اِلَيْهِ يَصْعَدُ الْكَلِمُ الطَّيِّبُ وَالْعَمَلُ الصَّالِحُ يَرْفَعُهٗ ؕ وَالَّذِيْنَ يَمْكُرُوْنَ السَّيِّاٰتِ لَهُمْ عَذَابٌ شَدِيْدٌ ؕ وَمَكْرُ اُولٰٓئِكَ هُوَ يَبُوْرُ ۝١٠

11. Anayeitaka heshima basi heshima yote ni ya Allah. Kwake hupanda maneno mazuri, kitendo kizuri huyapandisha. Na wale wanaopanga njama za maovu watapata adhabu kali na njama za watu hao zitaangamia.

وَاللّٰهُ خَلَقَكُمْ مِّنْ تُرَابٍ ثُمَّ مِنْ نُّطْفَةٍ ثُمَّ جَعَلَكُمْ اَزْوَاجًا ؕ وَمَا تَحْمِلُ مِنْ اُنْثٰى وَلَا تَضَعُ اِلَّا بِعِلْمِهٖ ؕ وَمَا يُعَمَّرُ مِنْ مُّعَمَّرٍ وَّلَا يُنْقَصُ مِنْ عُمُرِهٖٓ اِلَّا فِيْ كِتٰبٍ ؕ اِنَّ ذٰلِكَ عَلَى اللّٰهِ يَسِيْرٌ ۝١١

12. Na Allah Amewaumbeni kwa udongo, kisha kwa tone la manii, kisha Akawafanyeni jozi jozi. Na mwanamke ye yote hachukui mimba wala hazai ila kwa elimu Yake. Na mwenye kupewa umri hapewi umri (zaidi) wala hapunguziwi umri ila yamo Kitabuni. Bila shaka hayo ni rahisi kwa Allah.

وَمَا يَسْتَوِي الْبَحْرٰنِ ۖ هٰذَا عَذْبٌ فُرَاتٌ سَآئِغٌ شَرَابُهٗ وَهٰذَا مِلْحٌ اُجَاجٌ ؕ وَمِنْ

13. Na bahari mbili haziwi sawa: hii ni tamu yenye ladha, kinywaji chake chateremka upesi; na hii (nyingine) ni

Aya 13. Ikiwa watu wanaweza kupata vitu vizuri katika bahari tamu na bahari yenye

كُلٍّ تَاْكُلُوْنَ لَحْمًا طَرِيًّا وَّ تَسْتَخْرِجُوْنَ حِلْيَةً تَلْبَسُوْنَهَا ۚ وَتَرَى الْفُلْكَ فِيْهِ مَوَاخِرَ لِتَبْتَغُوْا مِنْ فَضْلِهٖ وَلَعَلَّكُمْ تَشْكُرُوْنَ ﴿١٢﴾

chumvi yenye uchungu; na katika zote mnakula nyama mbichi na mnatoa mapambo mnayovaa. Na ndani yake unaziona merikebu zikikata (maji) ili mtafute fadhili Yake na ili mpate kushukuru.

يُوْلِجُ الَّيْلَ فِي النَّهَارِ وَيُوْلِجُ النَّهَارَ فِي الَّيْلِ ۙ وَسَخَّرَ الشَّمْسَ وَالْقَمَرَ ۖ كُلٌّ يَّجْرِيْ لِاَجَلٍ مُّسَمًّى ؕ ذٰلِكُمُ اللّٰهُ رَبُّكُمْ لَهُ الْمُلْكُ ؕ وَالَّذِيْنَ تَدْعُوْنَ مِنْ دُوْنِهٖ مَا يَمْلِكُوْنَ مِنْ قِطْمِيْرٍ ﴿١٣﴾

14. Huingiza usiku katika mchana na huingiza mchana katika usiku, na Amevitiisha jua na mwezi, vyote vinapita mpaka muda maalumu. Huyo ndiye Allah, Mola wenu, Mwenye Ufalme; lakini wale mnaowaita kinyume Chake wao hawamiliki hata utando wa kokwa ya tende.

اِنْ تَدْعُوْهُمْ لَا يَسْمَعُوْا دُعَآءَكُمْ ۚ وَلَوْ سَمِعُوْا مَا اسْتَجَابُوْا لَكُمْ ؕ وَيَوْمَ الْقِيٰمَةِ يَكْفُرُوْنَ بِشِرْكِكُمْ ؕ وَلَا يُنَبِّئُكَ مِثْلُ خَبِيْرٍ ﴿١٤﴾

15. Kama mkiwaita hawasikii wito wenu; na kama wakisikia hawatawajibuni; na siku ya Kiyama wataikataa shirki yenu; wala (ye yote) hatakuambia kama (Aambiavyo Mungu) Mwenye habari.

FUNGU 3

يٰۤاَيُّهَا النَّاسُ اَنْتُمُ الْفُقَرَآءُ اِلَى اللّٰهِ ۚ وَاللّٰهُ هُوَ الْغَنِيُّ الْحَمِيْدُ ﴿١٥﴾

16. Enyi watu! ninyi ndio wenye haja kwa Allah, na Allah Ndiye Mkwasi (Asiyehitaji kwa yeyote), Asifiwaye.

اِنْ يَّشَاْ يُذْهِبْكُمْ وَيَاْتِ بِخَلْقٍ جَدِيْدٍ ﴿١٦﴾

17. Kama Akitaka Atawaondoeni na Ataleta viumbe wapya;

---

chumvi, vivyo hivyo maneno ya Allah pia yanaweza kuwatoa watu wazuri katika wabaya, na yana nguvu ya kuwafanya hata waliokuwa wabaya wawe wema. Jambo hili lilifanyika katika Uislamu, watoto wa makafiri wakubwa baadaye walishika Uislamu na wakawa watu wema sana; na watu waliokuwa wabaya waliingia Uislamu na kwa mafundisho ya Mtume *s.a.w.* na mfano wake mwema wakawa watu wema sana.

Aya 16. Mtu na awe tajiri namna gani atajiona kila siku na kila wakati anahitaji kwa Allah. Anahitaji kuvuta pumzi na kutoa pumzi, anahitaji kunywa na kwenda haja. Anahitaji kupata mwongozo na kutakasika. Ni nyingi bila idadi haja walizonazo watu kwa Allah.

وَمَا ذٰلِكَ عَلَى اللّٰهِ بِعَزِيْزٍ ﴿١٧﴾

18. Na jambo hili si gumu kwa Allah.

وَلَا تَزِرُ وَازِرَةٌ وِّزْرَ اُخْرٰى ؕ وَاِنْ تَدْعُ مُثْقَلَةٌ اِلٰى حِمْلِهَا لَا يُحْمَلْ مِنْهُ شَىْءٌ وَّلَوْ كَانَ ذَا قُرْبٰى ؕ اِنَّمَا تُنْذِرُ الَّذِيْنَ يَخْشَوْنَ رَبَّهُمْ بِالْغَيْبِ وَاَقَامُوا الصَّلٰوةَ ؕ وَمَنْ تَزَكّٰى فَاِنَّمَا يَتَزَكّٰى لِنَفْسِهٖ ؕ وَاِلَى اللّٰهِ الْمَصِيْرُ ﴿١٨﴾

19. Wala hatabeba mbebaji mzigo wa mwingine; na kama aliyelemewa na mzigo akimwitia (mwingine) mzigo wake hautachukuliwa hata kidogo hata kama yeye ni jamaa wa karibu. Hakika unawaonya wale tu wanaomwogopa Mola wao kwa siri na wanasimamisha Sala; na anayejitakasa, basi anajitakasa kwa ajili ya nafsi yake; na marudio ni kwa Allah.

وَمَا يَسْتَوِى الْاَعْمٰى وَالْبَصِيْرُ ﴿١٩﴾

20. Na kipofu na mwenye macho hawawi sawa.

وَلَا الظُّلُمٰتُ وَلَا النُّوْرُ ﴿٢٠﴾

21. Wala giza na nuru,

وَلَا الظِّلُّ وَلَا الْحَرُوْرُ ﴿٢١﴾

22. Wala kivuli na joto,

وَمَا يَسْتَوِى الْاَحْيَآءُ وَلَا الْاَمْوَاتُ ؕ اِنَّ اللّٰهَ يُسْمِعُ مَنْ يَّشَآءُ ۚ وَمَآ اَنْتَ بِمُسْمِعٍ مَّنْ فِى الْقُبُوْرِ ﴿٢٢﴾

23. Wala hawawi sawa wazima na wafu. Kwa yakini Allah Humsikilizisha Amtakaye, nawe huwezi kuwasikilizisha waliomo makaburini.

اِنْ اَنْتَ اِلَّا نَذِيْرٌ ﴿٢٣﴾

24. Wewe siye ila ni Mwonyaji tu.

اِنَّآ اَرْسَلْنٰكَ بِالْحَقِّ بَشِيْرًا وَّنَذِيْرًا ؕ وَاِنْ مِّنْ اُمَّةٍ اِلَّا خَلَا فِيْهَا نَذِيْرٌ ﴿٢٤﴾

25. Bila shaka Sisi Tumekutuma kwa haki ukiwa mwenye kutoa habari njema na mwonyaji, na hakuna taifa lo lote ila alipita humo Mwonyaji.

وَاِنْ يُّكَذِّبُوْكَ فَقَدْ كَذَّبَ الَّذِيْنَ مِنْ قَبْلِهِمْ ۚ جَآءَتْهُمْ رُسُلُهُمْ بِالْبَيِّنٰتِ وَبِالزُّبُرِ وَبِالْكِتٰبِ الْمُنِيْرِ ﴿٢٥﴾

26. Na kama wanakukadhibisha, basi walikwisha kadhibisha wale wa kabla yao: Mitume wao waliwafikia kwa dalili waziwazi na kwa maandiko na kwa Kitabu chenye nuru.

Aya 25. Aya hii inaonyesha ubora wa mafundisho ya Kiislamu. Qur'an inakubali ya kuwa kila taifa lilifikiwa na Mjumbe wa Allah. Mungu hakuwapendelea wengine na kuwaacha wengine; wote walikuwa na haja ya ufunuo wake na akawapelekea Mitume katika nyakati mbalimbali. Fundisho hili linaonyesha ya kuwa dini ya Kiislamu kweli imetoka kwa Allah, maana haina ubaguzi na kijicho na Mitume wa mataifa mengine na inawakubali wote.

27. Kisha Niliwakamata wale waliokufuru, basi adhabu Yangu ilikuwa (kali) namna gani!

ثُمَّ اَخَذْتُ الَّذِيْنَ كَفَرُوْا فَكَيْفَ كَانَ نَكِيْرِ ﴿٢٦﴾

FUNGU 4

28. Je, huoni kwamba Allah Ameteremsha maji kutoka mawinguni, na kwayo Tumeyatoa matunda yenye rangi mbalimbali: na katika milima imo mistari myeupe na myekundu yenye rangi mbalimbali, na (mingine) myeusi sana.

اَلَمْ تَرَ اَنَّ اللّٰهَ اَنْزَلَ مِنَ السَّمَآءِ مَآءً ۚ فَاَخْرَجْنَا بِهٖ ثَمَرٰتٍ مُّخْتَلِفًا اَلْوَانُهَا ؕ وَمِنَ الْجِبَالِ جُدَدٌۢ بِيْضٌ وَّحُمْرٌ مُّخْتَلِفٌ اَلْوَانُهَا وَغَرَابِيْبُ سُوْدٌ ﴿٢٧﴾

29. Na katika watu na viumbe watembeao ardhini, na wanyama pia rangi zao ni mbalimbali. Kwa hakika wamwogopao Allah miongoni mwa watumishi Wake ni wenye elimu. Bila shaka Allah ni Mwenye nguvu, Msamehevu.

وَمِنَ النَّاسِ وَالدَّوَآبِّ وَالْاَنْعَامِ مُخْتَلِفٌ اَلْوَانُهٗ كَذٰلِكَ ؕ اِنَّمَا يَخْشَى اللّٰهَ مِنْ عِبَادِهِ الْعُلَمٰٓؤُا ؕ اِنَّ اللّٰهَ عَزِيْزٌ غَفُوْرٌ ﴿٢٨﴾

30. Kwa yakini wale wanaosoma Kitabu cha Allah, na wanasimamisha Sala, na katika yale Tuliyowapa wanatoa kwa siri na kwa dhahiri, wanatumai biashara isiyoangamia.

اِنَّ الَّذِيْنَ يَتْلُوْنَ كِتٰبَ اللّٰهِ وَاَقَامُوا الصَّلٰوةَ وَاَنْفَقُوْا مِمَّا رَزَقْنٰهُمْ سِرًّا وَّعَلَانِيَةً يَّرْجُوْنَ تِجَارَةً لَّنْ تَبُوْرَ ﴿٢٩﴾

31. Ili Awape ujira wao sawasawa na kuwazidishia fadhili Zake. Hakika Yeye ni Msamehevu, Mwenye shukrani.

لِيُوَفِّيَهُمْ اُجُوْرَهُمْ وَيَزِيْدَهُمْ مِّنْ فَضْلِهٖ ؕ اِنَّهٗ غَفُوْرٌ شَكُوْرٌ ﴿٣٠﴾

32. Na ule wahyi tumeokuteremshia ndani ya Kitabu ndio haki, usadikishayo yaliyo mbele yake. Bila shaka Allah kwa watumishi Wake ni Mwenye habari, Mwenye kuona.

وَالَّذِيْٓ اَوْحَيْنَآ اِلَيْكَ مِنَ الْكِتٰبِ هُوَ الْحَقُّ مُصَدِّقًا لِّمَا بَيْنَ يَدَيْهِ ؕ اِنَّ اللّٰهَ بِعِبَادِهٖ لَخَبِيْرٌۢ بَصِيْرٌ ﴿٣١﴾

Aya 29. *Wenye elimu:* Ndio kusema, wenye elimu hasa wataonyesha ucha-Mungu katika mwenendo wao na tabia zao.

ثُمَّ اَوۡرَثۡنَا الۡكِتٰبَ الَّذِيۡنَ اصۡطَفَيۡنَا مِنۡ عِبَادِنَا‌ ۚ فَمِنۡهُمۡ ظَالِمٌ لِّنَفۡسِهٖ‌ ۚ وَمِنۡهُمۡ مُّقۡتَصِدٌ‌ ۚ وَمِنۡهُمۡ سَابِقٌۢ بِالۡخَيۡرٰتِ بِاِذۡنِ اللّٰهِ‌ ؕ ذٰلِكَ هُوَ الۡفَضۡلُ الۡكَبِيۡرُ ؕ﴿۳۲﴾

33. Kisha Tumekirithisha Kitabu kwa wale Tuliowachagua miongoni mwa watumishi Wetu. Basi yuko miongoni mwao anayejidhulumu nafsi yake, na yuko miongoni mwao anayeshika njia ya katikati, na yuko miongoni mwao anayepita mbele katika mema kwa idhini ya Allah. Hiyo ndiyo fadhili kubwa.

جَنّٰتُ عَدۡنٍ يَّدۡخُلُوۡنَهَا يُحَلَّوۡنَ فِيۡهَا مِنۡ اَسَاوِرَ مِنۡ ذَهَبٍ وَّلُؤۡلُؤًا‌ ۚ وَلِبَاسُهُمۡ فِيۡهَا حَرِيۡرٌ ﴿۳۳﴾

34. Mabustani ya milele watayaingia, humo watavikwa vikuku vya dhahabu, na lulu, na mavazi yao humo yatakuwa hariri.

وَقَالُوا الۡحَمۡدُ لِلّٰهِ الَّذِىۡۤ اَذۡهَبَ عَنَّا الۡحَزَنَ‌ ؕ اِنَّ رَبَّنَا لَغَفُوۡرٌ شَكُوۡرُ ۙ﴿۳۴﴾

35. Na watasema: Sifa zote njema ni za Allah Aliyetuondolea huzuni, kwa yakini Mola wetu ni Msamehevu, Mwenye shukurani,

الَّذِىۡۤ اَحَلَّنَا دَارَ الۡمُقَامَةِ مِنۡ فَضۡلِهٖ‌ ۚ لَا يَمَسُّنَا فِيۡهَا نَصَبٌ وَّلَا يَمَسُّنَا فِيۡهَا لُغُوۡبٌ ﴿۳۵﴾

36. Ambaye kwa fadhili Zake Ametuweka katika nyumba ya kukaa; humo haitugusi taabu wala humo hautugusi mchoko.

وَالَّذِيۡنَ كَفَرُوۡا لَهُمۡ نَارُ جَهَنَّمَ‌ ۚ لَا يُقۡضٰى عَلَيۡهِمۡ فَيَمُوۡتُوۡا وَلَا يُخَفَّفُ عَنۡهُمۡ مِّنۡ عَذَابِهَا‌ ؕ كَذٰلِكَ نَجۡزِىۡ كُلَّ كَفُوۡرٍ ﴿۳۶﴾

37. Na wale waliokufuru watakuwa na moto wa Jahanamu, hawatahukumiwa wapate kufa, wala hawatapunguziwa adhabu yake. Hivi ndivyo Tumlipavyo kila asiye na shukurani.

وَهُمۡ يَصۡطَرِخُوۡنَ فِيۡهَا‌ ۚ رَبَّنَاۤ اَخۡرِجۡنَا نَعۡمَلۡ صَالِحًا غَيۡرَ الَّذِىۡ كُنَّا نَعۡمَلُ‌ ؕ اَوَلَمۡ نُعَمِّرۡكُمۡ مَّا يَتَذَكَّرُ فِيۡهِ مَنۡ تَذَكَّرَ

38. Nao humo watalia: Mola wetu! Ututoe, tutafanya vitendo vizuri ghairi ya vile tulivyokuwa tukifanya. Je, Hatukuwapeni umri mwingi ili humo

Aya 33. Watu wanaopokea maagiza ya Allah wanapita katika madaraja matatu: Kwanza wanajilazimisha kuacha matamanio ya nafsi zao na wanajidhulumu sana na kufanya juhudi ya kuacha mazoea na matamanio ili kufuata maagizo ya Allah. Kisha wanafikia hali ya katikati na hawaoni taabu kama ile waliyoiona mwanzo. Na mwisho wanazoea kabisa na wema unakuwa ndiyo tabia yao na wanaona raha ndani yake.

Aya 35. *Mwenye shukurani,* yaani Allah haachi wema wa mtu ukapotea bure na analipa shukurani za watu kwa ukarimu sana.

وَجَآءَكُمُ النَّذِيْرُ ؕ فَذُوْقُوْا فَمَا لِلظّٰلِمِيْنَ مِنْ نَّصِيْرٍ ﴿۳۷﴾ ع ۱۶

akumbuke mwenye kutaka kukumbuka, na aliwafikieni Mwonyaji? Basi onjeni tu; na hakuna msaidizi kwa ajili ya wadhalimu.

FUNGU 5

اِنَّ اللّٰهَ عٰلِمُ غَيْبِ السَّمٰوٰتِ وَالْاَرْضِ ؕ اِنَّهٗ عَلِيْمٌۢ بِذَاتِ الصُّدُوْرِ ﴿۳۸﴾

39. Kwa hakika Allah ni Mjuzi wa siri za mbingu na ardhi; bila shaka Yeye ni Mjuzi wa yaliyomo vifuani.

هُوَ الَّذِيْ جَعَلَكُمْ خَلٰٓئِفَ فِي الْاَرْضِ ؕ فَمَنْ كَفَرَ فَعَلَيْهِ كُفْرُهٗ ؕ وَلَا يَزِيْدُ الْكٰفِرِيْنَ كُفْرُهُمْ عِنْدَ رَبِّهِمْ اِلَّا مَقْتًا ۚ وَلَا يَزِيْدُ الْكٰفِرِيْنَ كُفْرُهُمْ اِلَّا خَسَارًا ﴿۳۹﴾

40. Yeye ndiye Aliyewafanyeni manaibu katika ardhi; na anayekufuru, basi kufuru yake ni juu yake; na kufuru za makafiri haziwazidishii mbele ya Mola wao ila chuki, wala kufuru za makafiri haziwazidishii ila hasara.

قُلْ اَرَءَيْتُمْ شُرَكَآءَكُمُ الَّذِيْنَ تَدْعُوْنَ مِنْ دُوْنِ اللّٰهِ ؕ اَرُوْنِيْ مَاذَا خَلَقُوْا مِنَ الْاَرْضِ اَمْ لَهُمْ شِرْكٌ فِي السَّمٰوٰتِ ۚ اَمْ اٰتَيْنٰهُمْ كِتٰبًا فَهُمْ عَلٰى بَيِّنَتٍ مِّنْهُ ۚ بَلْ اِنْ يَّعِدُ الظّٰلِمُوْنَ بَعْضُهُمْ بَعْضًا اِلَّا غُرُوْرًا ﴿۴۰﴾

41. Sema: Mmewaona washirika wenu mnaowaita badala ya Allah? Nionyesheni ni sehemu ipi ya ardhi waliyoiumba au wanao ushirika katika mbingu? Au Tumewapa Kitabu nao kwa hicho wakawa na dalili waziwazi? Lakini wadhalimu hawaahidiani wao kwa wao ila udanganyifu.

اِنَّ اللّٰهَ يُمْسِكُ السَّمٰوٰتِ وَالْاَرْضَ اَنْ تَزُوْلَا ۚ وَلَئِنْ زَالَتَآ اِنْ اَمْسَكَهُمَا مِنْ اَحَدٍ مِّنْۢ بَعْدِهٖ ؕ اِنَّهٗ كَانَ حَلِيْمًا غَفُوْرًا ﴿۴۱﴾

42. Kwa yakini Allah Huzuia mbingu na ardhi zisiondoke; na kama zingedondoka, hakuna ye yote angezizuia baada Yake. Bila shaka Yeye ni Mpole mno, Msamehevu.

وَاَقْسَمُوْا بِاللّٰهِ جَهْدَ اَيْمَانِهِمْ لَئِنْ جَآءَهُمْ نَذِيْرٌ لَّيَكُوْنُنَّ اَهْدٰى مِنْ اِحْدَى الْاُمَمِ ۚ فَلَمَّا جَآءَهُمْ نَذِيْرٌ مَّا زَادَهُمْ اِلَّا نُفُوْرًا ۙ﴿۴۲﴾

43. Na waliapa kwa Allah kiapo chao kilicho kikubwa: akiwafikia Mwonyaji, bila shaka watakuwa katika waongofu zaidi kuliko taifa lingine lo lote. Lakini aliipowafikia Mwonyaji, basi hakuwazidishia ila chuki.

اسْتِكْبَارًا فِي الْاَرْضِ وَمَكْرَ السَّيِّئِ ؕ وَلَا يَحِيْقُ الْمَكْرُ السَّيِّئُ اِلَّا بِاَهْلِهٖ ؕ فَهَلْ يَنْظُرُوْنَ اِلَّا سُنَّتَ الْاَوَّلِيْنَ ۚ فَلَنْ تَجِدَ لِسُنَّتِ اللّٰهِ تَبْدِيْلًا ۖ وَلَنْ تَجِدَ لِسُنَّتِ اللّٰهِ تَحْوِيْلًا ﴿٤٣﴾

44. Na kujivuna ardhini, na (kufanya) hila mbaya; na hila mbaya haitamshika ila yule aliyeifanya. Basi je wao wanaingojea desturi yoyote ya Allah minghairi ya ile iliyowafikia watu wa zamani! Lakini hutapata mabadiliko katika kawaida ya Allah, wala hutakuta mageuko katika kawaida ya Allah.

اَوَلَمْ يَسِيْرُوْا فِي الْاَرْضِ فَيَنْظُرُوْا كَيْفَ كَانَ عَاقِبَةُ الَّذِيْنَ مِنْ قَبْلِهِمْ وَكَانُوْٓا اَشَدَّ مِنْهُمْ قُوَّةً ؕ وَمَا كَانَ اللّٰهُ لِيُعْجِزَهٗ مِنْ شَيْءٍ فِي السَّمٰوٰتِ وَلَا فِي الْاَرْضِ ؕ اِنَّهٗ كَانَ عَلِيْمًا قَدِيْرًا ﴿٤٤﴾

45. Je, hawakusafiri katika ardhi na kuona jinsi ulivyokuwa mwisho wa wale waliotangulia kabla yao, ilhali walikuwa wenye nguvu zaidi kuliko wao? na hakuna kitu kiwezacho kumshinda Allah, mbinguni wala ardhini. Bila shaka Yeye ni Mwenye kujua, Mwenye uwezo.

وَلَوْ يُؤَاخِذُ اللّٰهُ النَّاسَ بِمَا كَسَبُوْا مَا تَرَكَ عَلٰى ظَهْرِهَا مِنْ دَآبَّةٍ وَّلٰكِنْ يُّؤَخِّرُهُمْ اِلٰٓى اَجَلٍ مُّسَمًّى ۚ فَاِذَا جَآءَ اَجَلُهُمْ فَاِنَّ اللّٰهَ كَانَ بِعِبَادِهٖ بَصِيْرًا ﴿٤٥﴾ ع

46. Na kama Allah Angaliwakamata watu kwa sababu ya yale waliyoyachuma, Asingaliacha kiumbe chochote kitembeacho ardhini. Lakini Yeye Anawaakhirisha mpaka muda maalum. Basi muda wao uliokadiriwa utakapofika (itadhihirika wazi kwamba) Allah ni Mwenye kuwaona sana watumishi Wake.

Aya 44. *Makras-sayyi-i* "hila mbaya." Neno *makr* kwa Kiarabu maana yake ni hila tu, si hila nzuri wala mbaya. Hivyo imesemwa *makras-sayyi-i* kuonyesha ya kuwa hila za makafiri zilikuwa mbaya.

سُوْرَةُ يٰسٓ مَكِّيَّةٌ وَّ هِيَ مَعَ الْبَسْمَلَةِ اَرْبَعٌ وَّ ثَمَانُوْنَ اٰيَةً وَّ خَمْسَةُ رُكُوْعَاتٍ

36. SURA YAA SIIN

Imeteremshwa Makka

Ina mafungu 5 na Aya 84 pamoja na Bismillahi

بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ ①

1. Kwa jina la Allah, Mwingi wa rehema, Mwingi wa ukarimu.

يٰسٓ ②

2. Yaa sayyid, Ewe Kiongozi!

وَالْقُرْاٰنِ الْحَكِيْمِ ③

3. Naapa kwa Qur'an yanye hekima.

اِنَّكَ لَمِنَ الْمُرْسَلِيْنَ ④

4. Hakika wewe u miongoni mwa Waliotumwa,

عَلٰى صِرَاطٍ مُّسْتَقِيْمٍ ⑤

5. Juu ya njia iliyonyooka.

تَنْزِيْلَ الْعَزِيْزِ الرَّحِيْمِ ⑥

6. Ni uteremsho wa Mwenye ushindi kamili, Mrehemevu,

Sura hii ilishuka Makka na imesemwa ya kuwa makafiri waliposema Mtume Muhammad *s.a.w.* hakutumwa na Mungu, bali yeye ni yatima tu wa Abi Talib, asiyejua kusoma wala kuandika, Allah aliteremsha sura hii ya kutoa majibu na kuhakikisha unabii wake kwa kusema, *Hakika wewe u miongoni mwa waliotumwa.*

Mtume Muhammad *s.a.w.* amesema, "Kila kitu kinakuwa na moyo, na moyo wa Qur'an ni *Yaa Siin"* (Sawi). Tena Mtume *s.a.w*. alisema, "Mwislamu mwanamume au mwanamke anapokuwa katika hali ya kufa, basi asomewe sura *Yaa Siin,* na kwa kila neno wanashuka Malaika kumi wanaosimama mbele ya mgonjwa na kumsalia na kumwombea ghofira." Toka siku za Mtume *s.a.w* mpaka leo ni desturi ya Kiislamu kuwasomea sura *Yaa Siin* wagonjwa wanaokaribia kufa.

Aya 2. *Yaa Siin*, "Ewe mwanadamu mkamilifu." Herufi *Siin* ni kifupisho ama cha *Seyid* (Mkuu), au *Rasuul* (Mtume), au *Insaanul-kaamil* (mwanadamu mkamilifu). Hivyo Yaa Siin maana yake itakuwa, "Ewe Mkuu," "Ewe Mtume" na "Ewe mwanadamu mkamilifu." Maneno haya yanamhusu Mtume Muhammad *s.a.w.*

Aya 3. *Naapa.* Hapa tutaeleza habari kidogo juu ya viapo vya Allah vilivyomo katika Qur'an. Mwanadamu huapa kwa kutaka kukubalisha jambo lake, ambalo hakuna mtu aliyelishuhudia, basi anamfanya Mungu kuwa Shahidi.

Desturi ya Qur'an huanza kutoa kiapo kisha ikaleta madai. Kitu kile kinachoapiwa ndicho hufanywa shahidi wa kuhakikisha kuwa madai yanayotolewa ni ya haki. Mathalan katika Aya hii Allah anasema, "Naapa kwa Qur'an yenye hekima." Hapa Qur'an yenye hekima imefanywa shahidi kuhakikisha ya kuwa, "Hakika wewe (Muhammad) u miongoni mwa Waliotumwa." Ndiyo kusema mtu akisoma Qur'an, hekima ya mafundisho yake itamhakikishia ya kuwa asiyetumwa na Mungu hangeweza kuleta kitabu kama Qur'an, na hivyo Qur'an ni dalili ya kutosha kuhakikisha ya kuwa Muhammad s.a.w. ni Mjumbe wa Mwenyezi Mungu.

لِتُنْذِرَ قَوْمًا مَّآ اُنْذِرَ اٰبَآؤُهُمْ فَهُمْ غٰفِلُوْنَ ۝٦

7. Ili uwaonye watu ambao hawa-kuonywa baba zao, basi wao wameghafilika.

لَقَدْ حَقَّ الْقَوْلُ عَلٰٓى اَكْثَرِهِمْ فَهُمْ لَا يُؤْمِنُوْنَ ۝٧

8. Bila shaka kauli imehakiki juu ya wengi wao, kwa hiyo hawaamini.

اِنَّا جَعَلْنَا فِيْٓ اَعْنَاقِهِمْ اَغْلٰلًا فَهِيَ اِلَى الْاَذْقَانِ فَهُمْ مُّقْمَحُوْنَ ۝٨

9. Hakika Sisi Tumeweka minyororo shingoni mwao nayo inafika videvuni ndio sababu vichwa vyao vimetazamishwa juu.

وَجَعَلْنَا مِنْۢ بَيْنِ اَيْدِيْهِمْ سَدًّا وَّمِنْ خَلْفِهِمْ سَدًّا فَاَغْشَيْنٰهُمْ فَهُمْ لَا يُبْصِرُوْنَ ۝٩

10. Na Tumeweka kinga mbele yao na kinga nyuma yao na Tumewafunika, kwa hiyo hawaoni.

وَسَوَآءٌ عَلَيْهِمْ ءَاَنْذَرْتَهُمْ اَمْ لَمْ تُنْذِرْهُمْ لَا يُؤْمِنُوْنَ ۝١٠

11. Ni sawa kwao ukiwaonya au usiwaonye hawataamini.

اِنَّمَا تُنْذِرُ مَنِ اتَّبَعَ الذِّكْرَ وَخَشِيَ الرَّحْمٰنَ بِالْغَيْبِ ۚ فَبَشِّرْهُ بِمَغْفِرَةٍ وَّاَجْرٍ كَرِيْمٍ ۝١١

12. Unaweza tu kumwonya yule anayefuata mawaidha na akamwogopa Rahmani faraghani; basi mbashirie (kupata) msamaha na ujira wenye heshima.

اِنَّا نَحْنُ نُحْيِ الْمَوْتٰى وَنَكْتُبُ مَا قَدَّمُوْا وَاٰثَارَهُمْ ۭ وَكُلَّ شَيْءٍ اَحْصَيْنٰهُ فِيْٓ اِمَامٍ مُّبِيْنٍ ۝١٢

13. Kwa yakini Sisi Tunawahuisha wafu, na Tunayaandika waliyoyatanguli-za na athari zao, na kila kitu Tumekihi-fadhi katika daftari ibainishayo.

FUNGU 2

وَاضْرِبْ لَهُمْ مَّثَلًا اَصْحٰبَ الْقَرْيَةِ ۘ اِذْ جَآءَهَا الْمُرْسَلُوْنَ ۝١٣

14. Na uwapigie methali ya wenyeji wa mji Mitume walipoufikia.

اِذْ اَرْسَلْنَآ اِلَيْهِمُ اثْنَيْنِ فَكَذَّبُوْهُمَا فَعَزَّزْنَا بِثَالِثٍ فَقَالُوْٓا اِنَّآ اِلَيْكُمْ مُّرْسَلُوْنَ ۝١٤

15. Tulipowapelekea (mitume) wawili nao wakawakadhibisha, basi Tukawazidishia nguvu kwa (Mtume) wa tatu: nao walisema: Kwa yakini sisi tumetumwa kwenu.

Aya 10. *Tumeweka kinga mbele yao,* yaani mila zao zinawazuia kukubali Uislamu. Na *kinga nyuma yao* muradi wake, uasi wao utakuwa sababu ya kutia kutu nyoyo zao wazidi kuona vigumu kuikubali haki, na hivyo adhabu italazimika juu yao.

Aya 13. *Waliyoyatanguliza* ni matendo yao. *Nyayo zao* ni athari ya vitendo vyao inayobakia baada yao.

16. Wakasema: Ninyi si cho chote ila ni watu kama sisi, wala (Allah) Rahmani Hakuteremsha cho chote; ninyi mnasema uwongo tu.

قَالُوْا مَآ اَنْتُمْ اِلَّا بَشَرٌ مِّثْلُنَا ۙ وَمَآ اَنْزَلَ الرَّحْمٰنُ مِنْ شَيْءٍ ۙ اِنْ اَنْتُمْ اِلَّا تَكْذِبُوْنَ ﴿١٦﴾

17. Wakasema: Mola wetu Anajua bila shaka sisi tumetumwa kwenu.

قَالُوْا رَبُّنَا يَعْلَمُ اِنَّآ اِلَيْكُمْ لَمُرْسَلُوْنَ ﴿١٧﴾

18. Wala si juu yetu ila kufikisha (ujumbe) waziwazi.

وَمَا عَلَيْنَآ اِلَّا الْبَلٰغُ الْمُبِيْنُ ﴿١٨﴾

19. Wakasema: Hakika sisi tunapata mkosi kwa sababu yenu: kama hamtaacha kwa yakini tutawapigeni mawe, na bila shaka itawafikieni kutoka kwetu adhabu iumizayo.

قَالُوْٓا اِنَّا تَطَيَّرْنَا بِكُمْ ۚ لَئِنْ لَّمْ تَنْتَهُوْا لَنَرْجُمَنَّكُمْ وَلَيَمَسَّنَّكُمْ مِّنَّا عَذَابٌ اَلِيْمٌ ﴿١٩﴾

20. Wakasema: mkosi wenu u pamoja nanyi: je! kwa kuwa mnakumbushwa? Bali ninyi ni watu wapitao kiasi.

قَالُوْا طَآئِرُكُمْ مَّعَكُمْ ؕ اَئِنْ ذُكِّرْتُمْ ؕ بَلْ اَنْتُمْ قَوْمٌ مُّسْرِفُوْنَ ﴿٢٠﴾

21. Na akaja mtu mbio kutokea upande wa mbali wa mji, akasema: Enyi watu wangu, wafuateni Mitume.

وَجَآءَ مِنْ اَقْصَا الْمَدِيْنَةِ رَجُلٌ يَّسْعٰى قَالَ يٰقَوْمِ اتَّبِعُوا الْمُرْسَلِيْنَ ﴿٢١﴾

22. Wafuateni wasiowaombeni ujira; na hao wameongoka:

اتَّبِعُوْا مَنْ لَّا يَسْـَٔلُكُمْ اَجْرًا وَّهُمْ مُّهْتَدُوْنَ ﴿٢٢﴾

JUZU 23

23. Na nimekuwaje nisimwabudu Yule Aliyeniumba na Kwake mtarejeshwa?

وَمَا لِيَ لَآ اَعْبُدُ الَّذِيْ فَطَرَنِيْ وَاِلَيْهِ تُرْجَعُوْنَ ﴿٢٣﴾

24. Je, niwashike miungu badala Yake? Kama Rahmani Akipenda kunidhuru, uombezi wao hautanifaa kitu, wala hawataniokoa.

ءَاَتَّخِذُ مِنْ دُوْنِهٖٓ اٰلِهَةً اِنْ يُّرِدْنِ الرَّحْمٰنُ بِضُرٍّ لَّا تُغْنِ عَنِّيْ شَفَاعَتُهُمْ شَيْـًٔا وَّلَا يُنْقِذُوْنِ ﴿٢٤﴾

25. Kwa yakini ndipo nitakuwemo katika upotevu ulio wazi.

اِنِّيْٓ اِذًا لَّفِيْ ضَلٰلٍ مُّبِيْنٍ ﴿٢٥﴾

26. Bila shaka nimemwamini Mola wenu, basi nisikilizeni.

اِنِّيْٓ اٰمَنْتُ بِرَبِّكُمْ فَاسْمَعُوْنِ ﴿٢٦﴾

Imaamimmubiin, "Daftari ibainishayo," pia maana yake ni "Kitabu kilicho wazi, au daftari yenye hesabu ya vitendo vya watu.

قِيْلَ ادْخُلِ الْجَنَّةَ ؕ قَالَ يٰلَيْتَ قَوْمِيْ يَعْلَمُوْنَ ۙ﴿۲۷﴾

27. Ikasemwa: Ingia Peponi. Akasema: Laiti watu wangu wangejua.

بِمَا غَفَرَ لِيْ رَبِّيْ وَجَعَلَنِيْ مِنَ الْمُكْرَمِيْنَ﴿۲۸﴾

28. Jinsi Mola wangu Alivyonisamehe na Akanijaalia kuwa miongoni mwa walioheshimiwa.

وَمَاۤ اَنْزَلْنَا عَلٰى قَوْمِهٖ مِنْۢ بَعْدِهٖ مِنْ جُنْدٍ مِّنَ السَّمَآءِ وَمَا كُنَّا مُنْزِلِيْنَ﴿۲۹﴾

29. Na Hatukuwateremshia watu wake jeshi kutoka mbinguni baada yake, wala Hatukuwa Wateremshao.

اِنْ كَانَتْ اِلَّا صَيْحَةً وَّاحِدَةً فَاِذَا هُمْ خٰمِدُوْنَ﴿۳۰﴾

30. Haikuwa ila mlio mmoja tu, na mara wakawa waliozimika.

يٰحَسْرَةً عَلَى الْعِبَادِ ۚ مَا يَاْتِيْهِمْ مِّنْ رَّسُوْلٍ اِلَّا كَانُوْا بِهٖ يَسْتَهْزِءُوْنَ﴿۳۱﴾

31. Ni sikitiko kwa watumishi: hakuwafikia Mtume ye yote ila walikuwa wanamfanyia mzaha.

اَلَمْ يَرَوْا كَمْ اَهْلَكْنَا قَبْلَهُمْ مِّنَ الْقُرُوْنِ اَنَّهُمْ اِلَيْهِمْ لَا يَرْجِعُوْنَ ؕ﴿۳۲﴾

32. Je, hawaoni vizazi vingapi Tuliviangamiza kabla yao, hakika wao hawarejei kwao?

وَاِنْ كُلٌّ لَّمَّا جَمِيْعٌ لَّدَيْنَا مُحْضَرُوْنَ ۧ﴿۳۳﴾

33. Na hapana (atakayebaki) ila wote watahudhurishwa mbele Yetu.

FUNGU 3

وَاٰيَةٌ لَّهُمُ الْاَرْضُ الْمَيْتَةُ ۚ اَحْيَيْنٰهَا وَاَخْرَجْنَا مِنْهَا حَبًّا فَمِنْهُ يَاْكُلُوْنَ﴿۳۴﴾

34. Na Ishara kwa ajili yao ni ardhi iliyokufa: Twaifufua na Tukatoa ndani yake nafaka nayo wanaila.

وَجَعَلْنَا فِيْهَا جَنّٰتٍ مِّنْ نَّخِيْلٍ وَّاَعْنَابٍ وَّفَجَّرْنَا فِيْهَا مِنَ الْعُيُوْنِ ۙ﴿۳۵﴾

35. Na Twafanya ndani yake mabustani ya mitende na mizabibu na kupitisha chemchem ndani yake,

لِيَاْكُلُوْا مِنْ ثَمَرِهٖ ۙ وَمَا عَمِلَتْهُ اَيْدِيْهِمْ ؕ اَفَلَا يَشْكُرُوْنَ﴿۳۶﴾

36. Ili wale katika matunda yake; na yale iliyoyafanya mikono yao; je, hawashukuru?

Aya 29. *Jund,* "Jeshi" Neno hili pia limetolewa kwa maana ya "neema" (Akrab).

Aya 31. Hapa imeelezwa desturi ya watu. Kila mara anapowafikia Nabii wanamfanyia mzaha na kumwona kuwa hafifu.

Aya 34. Hapa "kifo" cha watu katika mambo ya kiroho na ustaarabu kimefananishwa na kifo cha ardhi. Juu ya kufa kwake, mara ikipata maji inakuwa hai na inatoa mazao. Hivyo ingawa Waarabu walikuwa katika namna ya kifo, lakini kwa mafunzo yaliyotereshwa katika ufunuo wa Mungu wakawa watu wema wenye kueneza elimu na ustaarabu. Hii ndiyo Ishara mojawapo inayohakikisha ya kuwa ingekuwa dini hii haikutoka kwa Mungu isingeweza kuleta mabadiliko ya namna hii.

سُبْحٰنَ الَّذِیْ خَلَقَ الْاَزْوَاجَ كُلَّهَا مِمَّا تُنْۢبِتُ الْاَرْضُ وَ مِنْ اَنْفُسِهِمْ وَ مِمَّا لَا یَعْلَمُوْنَ ﴿۳۶﴾

37. Mtukufu ni Yule Aliyeumba jozi za (vitu) vyote katika vile ivioteshavyo ardhi, na katika nafsi zao, na katika vile wasivyovijua.

وَ اٰیَةٌ لَّهُمُ الَّیْلُ ۖۚ نَسْلَخُ مِنْهُ النَّهَارَ فَاِذَا هُمْ مُّظْلِمُوْنَ ﴿۳۷﴾

38. Na Ishara kwa ajili yao ni usiku ambapo kutoka humo tunauvuta mchana na mara wao wamo gizani.

وَ الشَّمْسُ تَجْرِیْ لِمُسْتَقَرٍّ لَّهَا ؕ ذٰلِكَ تَقْدِیْرُ الْعَزِیْزِ الْعَلِیْمِ ﴿۳۸﴾

39. Na jua linapita katika njia iliyopangwa kwa ajili yake. Hiyo ndiyo Kudra ya Mwenye ushindi kamili, Mjuzi wa kila kitu.

وَ الْقَمَرَ قَدَّرْنٰهُ مَنَازِلَ حَتّٰى عَادَ كَالْعُرْجُوْنِ الْقَدِیْمِ ﴿۳۹﴾

40. Na mwezi Tumeupimia vituo mpaka unarudia kuwa kama kole la mtende la zamani.

لَا الشَّمْسُ یَنْۢبَغِیْ لَهَاۤ اَنْ تُدْرِكَ الْقَمَرَ وَ لَا الَّیْلُ سَابِقُ النَّهَارِ ؕ وَ كُلٌّ فِیْ فَلَكٍ یَّسْبَحُوْنَ ﴿۴۰﴾

41. Jua haliwezi kuufikia mwezi, wala usiku hauwezi kuupita mchana, na vyote huzunguka katika mhimili.

وَ اٰیَةٌ لَّهُمْ اَنَّا حَمَلْنَا ذُرِّیَّتَهُمْ فِی الْفُلْكِ الْمَشْحُوْنِ ﴿۴۱﴾

42. Na ni Ishara kwao ya kuwa Tumewapandisha wazao wao ndani ya safina iliyosheheni.

وَ خَلَقْنَا لَهُمْ مِّنْ مِّثْلِهٖ مَا یَرْكَبُوْنَ ﴿۴۲﴾

43. Na Tutawaumbia mfano wa hivi ambavyo watavipanda.

وَ اِنْ نَّشَاْ نُغْرِقْهُمْ فَلَا صَرِیْخَ لَهُمْ وَ لَا هُمْ یُنْقَذُوْنَ ﴿۴۳﴾

44. Na kama Tungetaka Tungewagharikisha, wala hangekuwapo wa kuwasaidia, wala wasingeokolewa.

اِلَّا رَحْمَةً مِّنَّا وَ مَتَاعًا اِلٰى حِیْنٍ ﴿۴۴﴾

45. Ila kwa rehema zitokazo Kwetu na kufaidisha kwa muda kidogo.

وَ اِذَا قِیْلَ لَهُمُ اتَّقُوْا مَا بَیْنَ اَیْدِیْكُمْ وَ مَا خَلْفَكُمْ لَعَلَّكُمْ تُرْحَمُوْنَ ﴿۴۵﴾

46. Na wanapoambiwa: Ogopeni yaliyoko mbele yenu na yaliyoko nyuma yenu huenda mtarehemiwa.

Aya 37. Aya hii inaonyesha jambo kubwa la maarifa ambalo lilikuwa halijulikani kwa watu isipokuwa katika zama hizi ilipopanuka elimu, ya kuwa kila kitu kiko katika jozi.

Aya 40. Mwezi unapokuwa mwembamba hufanana na kole la mtende lililokauka.

Aya 41. *Falak* ni njia zinamopita nyota na sayari angani katika mizunguko yao.

وَمَا تَاْتِيْهِمْ مِّنْ اٰيَةٍ مِّنْ اٰيٰتِ رَبِّهِمْ اِلَّا كَانُوْا عَنْهَا مُعْرِضِيْنَ ﴿٤٦﴾

47. Na haiwafikii Ishara yo yote katika Ishara za Mola wao ila huwa wenye kuipuuza.

وَاِذَا قِيْلَ لَهُمْ اَنْفِقُوْا مِمَّا رَزَقَكُمُ اللّٰهُ ۙ قَالَ الَّذِيْنَ كَفَرُوْا لِلَّذِيْنَ اٰمَنُوْٓا اَنُطْعِمُ مَنْ لَّوْ يَشَآءُ اللّٰهُ اَطْعَمَهٗٓ ۖ اِنْ اَنْتُمْ اِلَّا فِيْ ضَلٰلٍ مُّبِيْنٍ ﴿٤٧﴾

48. Na wanapoambiwa toeni katika yale Aliyowapeni Allah, wale waliokufuru huwaambia walioamini: Je, tumlishe ambaye Allah Angependa Angemlisha? Ninyi hammo ila katika upotevu dhahiri.

وَيَقُوْلُوْنَ مَتٰى هٰذَا الْوَعْدُ اِنْ كُنْتُمْ صٰدِقِيْنَ ﴿٤٨﴾

49. Na wanasema: Ahadi hii itatokea lini ikiwa mnasema kweli?

مَا يَنْظُرُوْنَ اِلَّا صَيْحَةً وَّاحِدَةً تَاْخُذُهُمْ وَهُمْ يَخِصِّمُوْنَ ﴿٤٩﴾

50. Hawangojei ila mlio mmoja utakaowashika, nao watakuwa katika hali ya kugombana;

فَلَا يَسْتَطِيْعُوْنَ تَوْصِيَةً وَّلَآ اِلٰٓى اَهْلِهِمْ يَرْجِعُوْنَ ﴿٥٠﴾ ع ٣

51. Na hawataweza kuusia wala kurejea kwa ahali zao.

FUNGU 4

وَنُفِخَ فِي الصُّوْرِ فَاِذَا هُمْ مِّنَ الْاَجْدَاثِ اِلٰى رَبِّهِمْ يَنْسِلُوْنَ ﴿٥١﴾

52. Na itapigwa baragumu, ndipo watatoka makaburini kwenda mbio-mbio kwa Mola wao.

قَالُوْا يٰوَيْلَنَا مَنْۢ بَعَثَنَا مِنْ مَّرْقَدِنَا ۜ هٰذَا مَا وَعَدَ الرَّحْمٰنُ وَصَدَقَ الْمُرْسَلُوْنَ ﴿٥٢﴾

53. Watasema, Ole wetu! nani ametufufua malaloni petu? Haya ndiyo Aliyoahidi Rahmani, na Waliotumwa walisema kweli.

اِنْ كَانَتْ اِلَّا صَيْحَةً وَّاحِدَةً فَاِذَا هُمْ جَمِيْعٌ لَّدَيْنَا مُحْضَرُوْنَ ﴿٥٣﴾

54. Haitakuwa ila mlio mmoja ndipo wote watahudhurishwa mbele Yetu.

فَالْيَوْمَ لَا تُظْلَمُ نَفْسٌ شَيْـًٔا وَّلَا تُجْزَوْنَ اِلَّا مَا كُنْتُمْ تَعْمَلُوْنَ ﴿٥٤﴾

55. Basi leo nafsi haitadhulumiwa cho chote wala hamtalipwa ila yale mliyokuwa mkitenda.

اِنَّ اَصْحٰبَ الْجَنَّةِ الْيَوْمَ فِيْ شُغُلٍ فٰكِهُوْنَ ﴿٥٥﴾ ج

56. Kwa yakini watu wa Peponi siku ile watafurahi wakijishughulisha na kazi mbalimbali;

هُمْ وَاَزْوَاجُهُمْ فِيْ ظِلٰلٍ عَلَى الْاَرَآئِكِ مُتَّكِـُٔوْنَ ﴿٥٦﴾

57. Wao na wake zao, katika vivuli wakiegemea juu ya viti vya fahari.

Aya 51. Mradi wa Aya hii ni kwamba itawafikia adhabu ya ghafla hata hawatakuwa na nafasi ya kuusia cho chote au kufanya mpango wo wote utakaoweza kuendeshwa baada yao. Adhabu ya namna hii iliwafikia makafiri wakubwa walipohiliki katika vita vya Badri.

لَهُمْ فِيْهَا فَاكِهَةٌ وَّلَهُمْ مَّا يَدَّعُوْنَ ﴿٥٧﴾

58. Yatakuwamo matunda kwa ajili yao na watapata watakavyovitaka.

سَلٰمٌ ۚ قَوْلًا مِّنْ رَّبٍّ رَّحِيْمٍ ﴿٥٨﴾

59. Salaam - ndiyo kauli itokayo kwa Mola Mwenye rehema.

وَامْتَازُوا الْيَوْمَ اَيُّهَا الْمُجْرِمُوْنَ ﴿٥٩﴾

60. Na jitengeni leo enyi wakosefu!

اَلَمْ اَعْهَدْ اِلَيْكُمْ يٰبَنِيْۤ اٰدَمَ اَنْ لَّا تَعْبُدُوا الشَّيْطٰنَ ۚ اِنَّهٗ لَكُمْ عَدُوٌّ مُّبِيْنٌ ﴿٦٠﴾

61. Je, Sikuwaagizeni enyi wanadamu msimwabudu Shetani? Hakika yeye ni adui bayana kwenu.

وَّاَنِ اعْبُدُوْنِيْ ؕ هٰذَا صِرَاطٌ مُّسْتَقِيْمٌ ﴿٦١﴾

62. Na ya kwamba mniabudu Mimi; hii ndiyo njia iliyonyoka.

وَلَقَدْ اَضَلَّ مِنْكُمْ جِبِلًّا كَثِيْرًا ؕ اَفَلَمْ تَكُوْنُوْا تَعْقِلُوْنَ ﴿٦٢﴾

63. Na bila shaka amewapoteza viumbe wengi miongoni mwenu; je, hamkuwa mkifikiri?

هٰذِهٖ جَهَنَّمُ الَّتِيْ كُنْتُمْ تُوْعَدُوْنَ ﴿٦٣﴾

64. Hii ndiyo Jahanamu mliyokuwa mkiahidiwa.

اِصْلَوْهَا الْيَوْمَ بِمَا كُنْتُمْ تَكْفُرُوْنَ ﴿٦٤﴾

65. Leo iingieni kwa sababu mlikuwa mkikufuru.

اَلْيَوْمَ نَخْتِمُ عَلٰۤى اَفْوَاهِهِمْ وَتُكَلِّمُنَاۤ اَيْدِيْهِمْ وَتَشْهَدُ اَرْجُلُهُمْ بِمَا كَانُوْا يَكْسِبُوْنَ ﴿٦٥﴾

66. Siku hiyo Tutapiga mihuri juu ya vinywa vyao, na mikono yao itazungumza nasi, na miguu yao itatoa ushahidi kwa yale waliyokuwa wakiyachuma.

وَلَوْ نَشَآءُ لَطَمَسْنَا عَلٰۤى اَعْيُنِهِمْ فَاسْتَبَقُوا الصِّرَاطَ فَاَنّٰى يُبْصِرُوْنَ ﴿٦٦﴾

67. Na kama Tungependa Tungeyang'oa macho yao, basi wangeshindania (kufika kwanza katika) njia; lakini wangeonaje?

وَلَوْ نَشَآءُ لَمَسَخْنٰهُمْ عَلٰى مَكَانَتِهِمْ فَمَا اسْتَطَاعُوْا مُضِيًّا وَّلَا يَرْجِعُوْنَ ﴿٦٧﴾

68. Na kama Tungetaka Tungewaangamiza majumbani mwao, basi wasingeweza kutembea wala kurejea.

Aya 59. *Salaam.* Neno hili maana yake ni "amani." Nalo linaonyesha kwa jumla ya kuwa Pepo ya Waislamu itakuwa ya amani na utulivu.

Aya 66. Mikono kuzungumza na migu kutoa ushahidi si jambo la kutatanisha. Katika elimu ya utabibu mkono wa mtu humwambia daktari habari za kweli ambazo pengine mtu mwenyewe asingeweza kuzisema. Na kwa mwendo wake huweza kujulikana ugonjwa wake. Katika Akhera mambo yatakuwa wazi zaidi.

FUNGU 5

وَمَنْ نُّعَمِّرْهُ نُنَكِّسْهُ فِي الْخَلْقِ ؕ اَفَلَا يَعْقِلُوْنَ ﴿٦٨﴾

69. Na Tunayempa umri mrefu Tunamdhoofisha katika umbo. Basi je hawatumii akili?

وَمَا عَلَّمْنٰهُ الشِّعْرَ وَمَا يَنْۢبَغِيْ لَهٗ ؕ اِنْ هُوَ اِلَّا ذِكْرٌ وَّقُرْاٰنٌ مُّبِيْنٌ ﴿٦٩﴾ لِّيُنْذِرَ مَنْ كَانَ حَيًّا وَّيَحِقَّ الْقَوْلُ عَلَى الْكٰفِرِيْنَ ﴿٧٠﴾

70. Wala Hatukumfundisha shairi, wala haimpasi, huu siyo ila ni ukumbusho na Qur'an ibainishayo,

71. Ili amwonye aliye hai na ihakikike kauli juu ya makafiri.

اَوَلَمْ يَرَوْا اَنَّا خَلَقْنَا لَهُمْ مِّمَّا عَمِلَتْ اَيْدِيْنَاۤ اَنْعَامًا فَهُمْ لَهَا مٰلِكُوْنَ ﴿٧١﴾

72. Je, hawaoni ya kwamba Tumewaumbia, katika vile ilivyovifanya mikono Yetu, wanyama; nao wanawamiliki?

وَذَلَّلْنٰهَا لَهُمْ فَمِنْهَا رَكُوْبُهُمْ وَمِنْهَا يَاْكُلُوْنَ ﴿٧٢﴾

73. Na Tumewatiishia (wanyama) hao basi baadhi yao wanawapanda na wengine wao wanawala.

وَلَهُمْ فِيْهَا مَنَافِعُ وَمَشَارِبُ ؕ اَفَلَا يَشْكُرُوْنَ ﴿٧٣﴾

74. Na katika hao wanapata manufaa na vinywaji; basi je, hawashukuru?

وَاتَّخَذُوْا مِنْ دُوْنِ اللّٰهِ اٰلِهَةً لَّعَلَّهُمْ يُنْصَرُوْنَ ﴿٧٤﴾

75. Na wameshika miungu mingine badala ya Allah wapate kusaidiwa.

لَا يَسْتَطِيْعُوْنَ نَصْرَهُمْ ۙ وَهُمْ لَهُمْ جُنْدٌ مُّحْضَرُوْنَ ﴿٧٥﴾

76. Hawataweza kuwasaidia bali kinyume chake wao wenyewe watafanywa wawe pamoja na hao kama jeshi moja.

Aya 69. Hii ndiyo kanuni inayojulikana kabisa na isiyobadilika ya kuwa kinachopata umri mrefu kinapungua nguvu na kinachakaa. Kama Nabii Isa ni hai kwa miaka 2000, mnaweza kupimia wenyewe atafanya kazi gani na maisha yake hayo yana raha gani.

Aya 70. *Shi'ir.* Neno hili maana yake ni "shairi" au "uwongo" (Mufradat). Katika Aya hiii lina maana ya uwongo, maana kuna riwaya zinazoeleza ya kuwa Mtume *s.a.w.* alipata kusema shairi chache alizotunga mwenyewe: Kwa mfano, Mtume *s.a.w.* alisema.

Anannabiyyu la kadhib - Anabnu 'Abdil Muttalib yaani "Mimi ni Nabii si uwongo, mimi ni bin Abdil Muttali." Pia alisema:

Maa anti illa isba'un damiitii - Wa fii sabiilillaahi maa laqiitii. "Wewe si cho chote ila kidole uliyejeruhika. Na umepata haya katika njia ya Allah."

Kadhalika Mtume *s.a.w.* alisema, "Hakika katika baadhi ya shairi mna hekima" (Bukhari).

77. Basi isikuhuzunishe kauli yao; bila shaka Sisi Tunajua wanayoyaficha na wanayoyatangaza.

فَلَا يَحْزُنْكَ قَوْلُهُمْ ۘ اِنَّا نَعْلَمُ مَا يُسِرُّوْنَ وَ مَا يُعْلِنُوْنَ ﴿۷۷﴾

78. Je, mwanadamu hatambui ya kwamba Tumemwumba kwa tone la manii? Lakini lo! amekuwa hasimu dhahiri.

اَوَلَمْ يَرَ الْاِنْسَانُ اَنَّا خَلَقْنٰهُ مِنْ نُّطْفَةٍ فَاِذَا هُوَ خَصِيْمٌ مُّبِيْنٌ ﴿۷۸﴾

79. Na akatupigia mfano na kusahau umbo lake, akasema: Nani atakayeihuisha mifupa na hali imesagika?

وَضَرَبَ لَنَا مَثَلًا وَّ نَسِيَ خَلْقَهٗ ؕ قَالَ مَنْ يُّحْيِ الْعِظَامَ وَ هِيَ رَمِيْمٌ ﴿۷۹﴾

80. Sema: Ataihuisha Aliyeiumba mara ya kwanza, naye ni Mjuzi wa kila (namna ya) kuumba.

قُلْ يُحْيِيْهَا الَّذِيْۤ اَنْشَاَهَاۤ اَوَّلَ مَرَّةٍ ؕ وَ هُوَ بِكُلِّ خَلْقٍ عَلِيْمُ ۙ﴿۷۹﴾

81. Ambaye Amewafanyieni moto katika (mti) mbichi, ndipo nanyi huo mkauwasha.

الَّذِيْ جَعَلَ لَكُمْ مِّنَ الشَّجَرِ الْاَخْضَرِ نَارًا فَاِذَاۤ اَنْتُمْ مِّنْهُ تُوْقِدُوْنَ ﴿۸۰﴾

82. Je, Aliyeziumba mbingu na ardhi Hana uwezo wa kuumba mfano wao? Naam, naye ni Mwumbaji mkuu, Mjuzi.

اَوَلَيْسَ الَّذِيْ خَلَقَ السَّمٰوٰتِ وَ الْاَرْضَ بِقٰدِرٍ عَلٰۤى اَنْ يَّخْلُقَ مِثْلَهُمْ ؕ بَلٰى ۙ وَ هُوَ الْخَلّٰقُ الْعَلِيْمُ ﴿۸۱﴾

83. Hakika amri Yake Anapotaka cho chote Hukiambia, "Kuwa", basi kinaanza kuwa.

اِنَّمَاۤ اَمْرُهٗۤ اِذَاۤ اَرَادَ شَيْـًٔا اَنْ يَّقُوْلَ لَهٗ كُنْ فَيَكُوْنُ ﴿۸۲﴾

84. Basi Atukuzwe Yeye ambaye mkononi Mwake umo ufalme wa kila kitu, na Kwake mtarejea.

فَسُبْحٰنَ الَّذِيْ بِيَدِهٖ مَلَكُوْتُ كُلِّ شَيْءٍ وَّ اِلَيْهِ تُرْجَعُوْنَ ﴿۸۳﴾

سُوْرَةُ الصّٰٓفّٰتِ مَكِّيَّةٌ وَّ هِيَ مَعَ الْبَسْمَلَةِ مِائَةٌ وَّ ثَلَاثٌ وَّ ثَمَانُوْنَ اٰيَةً وَّخَمْسَةُ رُكُوْعَاتٍ

37. SURA AS-SAAFFAAT

Imetermshwa Makka

Ina mafungu 5 na Aya 183 pamoja na Bismillahi

بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ ۝١

1. Kwa jina la Allah, Mwingi wa rehema, Mwingi wa ukarimu.

وَالصّٰٓفّٰتِ صَفًّا ۝٢

2. Naapa kwa wajipangao safu-safu,

فَالزّٰجِرٰتِ زَجْرًا ۝٣

3. Tena kwa wale wazuiao sana,

فَالتّٰلِيٰتِ ذِكْرًا ۝٤

4. Kisha kwa wale wamtajao sana Allah,

اِنَّ اِلٰهَكُمْ لَوَاحِدٌ ۝٥

5. Kwa yakini Mungu wenu ni Mmoja tu:

رَبُّ السَّمٰوٰتِ وَالْاَرْضِ وَمَا بَيْنَهُمَا وَرَبُّ الْمَشَارِقِ ۝٦

6. Mola wa mbingu na ardhi na yaliyomo kati yao, na ni Mola wa mashariki zote.

اِنَّا زَيَّنَّا السَّمَآءَ الدُّنْيَا بِزِيْنَةِ ِۨالْكَوَاكِبِ ۝٧

7. Bila shaka Sisi Tumeipamba mbingu ya karibu kwa pambo la nyota,

وَحِفْظًا مِّنْ كُلِّ شَيْطٰنٍ مَّارِدٍ ۝٨

8. Na kuilinda na kila shetani muasi.

لَا يَسَّمَّعُوْنَ اِلَى الْمَلَاِ الْاَعْلٰى وَيُقْذَفُوْنَ مِنْ كُلِّ جَانِبٍ ۝٩

9. Hawataweza kuusikiliza mkutano mtukufu na watapigwa mawe toka kila upande.

دُحُوْرًا وَّلَهُمْ عَذَابٌ وَّاصِبٌ ۝١٠

10. Kwa kusukumwa; na wanayo adhabu idumuyo.

Jina la sura hii limetoka katika Aya ya 2. Sura hii ilishuka Makka.

Aya 2-4. Ni viapo ambavyo vinatangulizwa kama ilivyo desturi ya Qur'an kuweka ushahidi kisha kutoa madai ambayo hapa yanatokea katika Aya ya 5 ya kuwa Mungu wetu ni Mmoja tu.

Kama mikutano mikubwa mikubwa ifanywe, na watu wakae safu, na polisi wawekwe kuzuia isitokee fujo, kisha watu wakubwa-wakubwa wenye elimu watoe hotuba, baada ya kupeleleza mwishoni itahakikishwa ya kuwa Mungu ni Mmoja tu.

Aya 8. *Shaitaanimmariid.* Maneno haya tumeyafasiri "Shetani asi." Hawa walioitwa mashetani katika Aya hii, ni watu ambao Waarabu waliwaita "Kahin" yaani makuhani au waganga, ambao hawawafuati Manabii na wanajaribu kutafutafuta habari za ghaibu na za siri huko na huko.

Aya 9. *Mkutano mtukufu* ni mkutano wa Malaika Jibril na Malaika wengine wakubwa. Hawa makuhani hawana uwezo wa kusikiliza yanayopitishwa katika mikutano hiyo.

11. Isipokuwa anyakuaye unyakuzi, basi mara humfuata kimondo king'aacho.

إِلَّا مَنْ خَطِفَ الْخَطْفَةَ فَأَتْبَعَهُ شِهَابٌ ثَاقِبٌ ﴿١١﴾

12. Basi waulize iwapo wawezacho kukiumba ni chenye nguvu zaidi kuliko kile Tulichokiumba. Hao Tuliwaumba kwa udongo unatao.

فَاسْتَفْتِهِمْ أَهُمْ أَشَدُّ خَلْقًا أَمْ مَّنْ خَلَقْنَا ۚ إِنَّا خَلَقْنَاهُمْ مِّنْ طِينٍ لَّازِبٍ ﴿١٢﴾

13. Bali unastaajabu, na wao wanafanya mzaha.

بَلْ عَجِبْتَ وَيَسْخَرُونَ ﴿١٣﴾

14. Na wanapokumbushwa hawakumbuki.

وَإِذَا ذُكِّرُوا لَا يَذْكُرُونَ ﴿١٤﴾

15. Na wanapoiona Ishara hufanya mzaha.

وَإِذَا رَأَوْا آيَةً يَّسْتَسْخِرُونَ ﴿١٥﴾

16. Na wanasema: Siyo huu ila ni uchawi dhahiri.

وَقَالُوا إِنْ هَٰذَا إِلَّا سِحْرٌ مُّبِينٌ ﴿١٦﴾

17. Je, tutakapokufa na kuwa udongo na mifupa kweli tutafufuliwa?

أَإِذَا مِتْنَا وَكُنَّا تُرَابًا وَعِظَامًا أَإِنَّا لَمَبْعُوثُونَ ﴿١٧﴾

18. Hata baba zetu wa zamani?

أَوَآبَاؤُنَا الْأَوَّلُونَ ﴿١٨﴾

19. Sema: Naam, nanyi mtafedheheka.

قُلْ نَعَمْ وَأَنْتُمْ دَاخِرُونَ ﴿١٩﴾

20. Na hakika litakuwa kemeo moja tu, mara watatazama!

فَإِنَّمَا هِيَ زَجْرَةٌ وَاحِدَةٌ فَإِذَا هُمْ يَنْظُرُونَ ﴿٢٠﴾

21. Na watasema: Ole wetu! hii ni siku ya Malipo!

وَقَالُوا يَا وَيْلَنَا هَٰذَا يَوْمُ الدِّينِ ﴿٢١﴾

22. Hii ndiyo siku ya Hukumu ambayo mlikuwa mkiikadhibisha.

هَٰذَا يَوْمُ الْفَصْلِ الَّذِي كُنْتُمْ بِهِ تُكَذِّبُونَ ﴿٢٢﴾ ع

FUNGU 2

23. Wakusanyeni wale waliodhulumu na wenzi wao na wale waliokuwa wakiwaabudu,

احْشُرُوا الَّذِينَ ظَلَمُوا وَأَزْوَاجَهُمْ وَمَا كَانُوا يَعْبُدُونَ ﴿٢٣﴾

24. Badala ya Allah, na waongozeni kwenye njia ya Jahanamu.

مِنْ دُونِ اللَّهِ فَاهْدُوهُمْ إِلَىٰ صِرَاطِ الْجَحِيمِ ﴿٢٤﴾ ع

Aya 11. *Isipokuwa anyakuaye.* Hawa makuhani huweza kudakia alama ndogo-ndogo zinazoonekana na wakazipamba kwa maongezo yao, kisha wakazieleza kwa watu. Hapo Allah anadhihirisha Ishara ya nguvu kwa mkono wa Nabii na inakuwa kama kimondo kinachofukuza uaguzi wa makuhani na kudhihirisha uwongo wao.

وَقِفُوْهُمْ اِنَّهُمْ مَّسْـُٔوْلُوْنَ ﴿٢٥﴾

25. Na wasimamisheni, hakika wao wataulizwa.

مَا لَكُمْ لَا تَنَاصَرُوْنَ ﴿٢٦﴾

26. Mmekuwaje hamsaidiani?

بَلْ هُمُ الْيَوْمَ مُسْتَسْلِمُوْنَ ﴿٢٧﴾

27. Bali leo ni wenye kukiri (kila kosa).

وَاَقْبَلَ بَعْضُهُمْ عَلٰى بَعْضٍ يَّتَسَآءَلُوْنَ ﴿٢٨﴾

28. Nao wataelekeana wakiulizana.

قَالُوْٓا اِنَّكُمْ كُنْتُمْ تَاْتُوْنَنَا عَنِ الْيَمِيْنِ ﴿٢٩﴾

29. Watasema: Kwa hakika ninyi mlikuwa mkitufikia kwa upande wa kuume (upande wa dini ili mtupoteze).

قَالُوْا بَلْ لَّمْ تَكُوْنُوْا مُؤْمِنِيْنَ ﴿٣٠﴾

30. Watasema: Bali ninyi hamkuwa waaminio.

وَمَا كَانَ لَنَا عَلَيْكُمْ مِّنْ سُلْطٰنٍ ۚ بَلْ كُنْتُمْ قَوْمًا طٰغِيْنَ ﴿٣١﴾

31. Na hatukuwa na mamlaka juu yenu, bali ninyi mlikuwa watu waasi.

فَحَقَّ عَلَيْنَا قَوْلُ رَبِّنَا ۖ اِنَّا لَذَآئِقُوْنَ ﴿٣٢﴾

32. Basi hukumu ya Mola wetu ime-hakiki juu yetu, bila shaka tutaonja.

فَاَغْوَيْنٰكُمْ اِنَّا كُنَّا غٰوِيْنَ ﴿٣٣﴾

33. Tuliwapotezeni, hakika sisi tulikuwa wapotevu.

فَاِنَّهُمْ يَوْمَئِذٍ فِى الْعَذَابِ مُشْتَرِكُوْنَ ﴿٣٤﴾

34. Basi wao kwa hakika siku hiyo wote watashiriki sawasawa katika adhabu.

اِنَّا كَذٰلِكَ نَفْعَلُ بِالْمُجْرِمِيْنَ ﴿٣٥﴾

35. Hivyo ndivyo Tunavyofanya kwa wakosefu.

اِنَّهُمْ كَانُوْٓا اِذَا قِيْلَ لَهُمْ لَآ اِلٰهَ اِلَّا اللّٰهُ ۙ يَسْتَكْبِرُوْنَ ﴿٣٦﴾

36. Hakika wao, walipokuwa waki-ambiwa, Hakuna aabudiwaye isipokuwa Allah, walikuwa wakifanya kiburi.

وَيَقُوْلُوْنَ اَئِنَّا لَتَارِكُوْٓا اٰلِهَتِنَا لِشَاعِرٍ مَّجْنُوْنٍ ﴿٣٧﴾

37. Na husema: Je, tuiache miungu yetu kwa ajili ya mshairi majnuni?

بَلْ جَآءَ بِالْحَقِّ وَصَدَّقَ الْمُرْسَلِيْنَ ﴿٣٨﴾

38. Bali Ameleta haki na amewasadikisha Waliotumwa.

اِنَّكُمْ لَذَآئِقُوا الْعَذَابِ الْاَلِيْمِ ﴿٣٩﴾

39. Hakika ninyi bila shaka mtaionja adhabu iumizayo.

وَمَا تُجْزَوْنَ اِلَّا مَا كُنْتُمْ تَعْمَلُوْنَ ﴿٤٠﴾

40. Wala hamtalipwa ila yale mliyokuwa mkiyafanya.

اِلَّا عِبَادَ اللّٰهِ الْمُخْلَصِيْنَ ﴿٤١﴾

41. Isipokuwa watumishi wa Allah waliohalisika.

اُولٰٓئِكَ لَهُمْ رِزْقٌ مَّعْلُوْمٌ ﴿٤٢﴾

42. Hao ndio watapata riziki maalumu,

فَوَاكِهُ ۚ وَهُمْ مُّكْرَمُوْنَ ﴿٤٢﴾

43. Matunda na wao wataheshimiwa.

فِيْ جَنّٰتِ النَّعِيْمِ ﴿٤٣﴾

44. Katika Bustani zenye neema.

عَلٰى سُرُرٍ مُّتَقٰبِلِيْنَ ﴿٤٤﴾

45. Juu ya vitanda vya fahari wakikabiliana.

يُطَافُ عَلَيْهِمْ بِكَاْسٍ مِّنْ مَّعِيْنٍ ﴿٤٥﴾

46. Wakizungushiwa kikombe chenye (kinywaji) safi,

بَيْضَآءَ لَذَّةٍ لِّلشّٰرِبِيْنَ ﴿٤٦﴾

47. Cheupe, chenye ladha kwa wanywao.

لَا فِيْهَا غَوْلٌ وَّلَا هُمْ عَنْهَا يُنْزَفُوْنَ ﴿٤٧﴾

48. Ndani ya (vinywaji hivyo) hautakuwamo ulevi na wala athari zake hazitaziharibu akili zao.

وَعِنْدَهُمْ قٰصِرٰتُ الطَّرْفِ عِيْنٌ ﴿٤٨﴾

49. Na watakuwa na wanawake wenye macho mazuri na makubwa yatazamayo chini.

كَاَنَّهُنَّ بَيْضٌ مَّكْنُوْنٌ ﴿٤٩﴾

50. (Yatang'aa) kana kwamba ni mayai yaliyohifadhiwa.

فَاَقْبَلَ بَعْضُهُمْ عَلٰى بَعْضٍ يَّتَسَآءَلُوْنَ ﴿٥٠﴾

51. Tena wataelekeana wao kwa wao wakiulizana.

قَالَ قَآئِلٌ مِّنْهُمْ اِنِّيْ كَانَ لِيْ قَرِيْنٌ ﴿٥١﴾

52. Atasema msemaji miongoni mwao: Hakika nilikuwa na rafiki.

يَّقُوْلُ اَئِنَّكَ لَمِنَ الْمُصَدِّقِيْنَ ﴿٥٢﴾

53. Aliyesema: Je, wewe ni katika wale wanaosadikisha?

ءَاِذَا مِتْنَا وَكُنَّا تُرَابًا وَّعِظَامًا ءَاِنَّا لَمَدِيْنُوْنَ ﴿٥٣﴾

54. Je, tutakapokufa na tutakuwa udongo na mifupa tutahukumiwa?

قَالَ هَلْ اَنْتُمْ مُّطَّلِعُوْنَ ﴿٥٤﴾

55. Atasema: Je, mtaweza kuchungulia?

فَاطَّلَعَ فَرَاٰهُ فِيْ سَوَآءِ الْجَحِيْمِ ﴿٥٥﴾

56. Basi akachungulia na akamwona katikati ya Jahanamu.

قَالَ تَاللّٰهِ اِنْ كِدْتَّ لَتُرْدِيْنِ ﴿٥٦﴾

57. Naye atasema: Wallahi ulikuwa karibu kuniangamiza.

وَلَوْلَا نِعْمَةُ رَبِّيْ لَكُنْتُ مِنَ الْمُحْضَرِيْنَ ﴿٥٧﴾

58. Na lau si neema ya Mola wangu, bila shaka ningalikuwa miongoni mwa waliohudhurishwa.

Aya 50. *Baidhun* ni sawasawa na *baidhatun*. Ni yai la mbuni au la ndege yo yote. Inaposemwa katika kumsifia mtu huwa *baidhatul balad* ina maana kwamba: Yeye ni kama yai la mbuni ambalo ndani yake mna kifaranga, kwani jogoo la mbuni ndilo linalolilinda yai hilo; au hana mwenzake katika ubora kama lile yai linaloachwa peke yake; au ni mwinyi au chifu au asiye na wa kulingana naye katika ile *balad* (nchi au mahali) ambapo wanaishi watu wengine, na ambaye maneno yake yanakubalika na wote, au ni mwenye kutukuzwa au mwenye kujulikana sana. Hivyo basi *baidhun maknuun* itakuwa na maana ya fahari ya pepo yenye kulindwa na kuhifadhiwa vizuri sana.

59. Je, sisi hatutakufa,

60. Ila kifo chetu cha kwanza? Wala hatutaadhibiwa?

61. Bila shaka huo ndiyo ufaulu mkuu.

62. Basi wafanyao wafanye sawa na mfano huu.

63. Je, karibisho la namna hii ni bora au mti wa zakkum?

64. Kwa yakini Sisi Tumeufanya jaribio kwa wadhalimu.

65. Hakika huo ni mti uotao katikati ya Jahanamu.

66. Matunda yake ni kama vichwa vya mashetani.

67. Bila shaka wao watakula katika huo, na kwa huo watajaza matumbo.

68. Kisha bila shaka watapewa juu ya huo mchanganyiko wa maji ya moto.

69. Halafu kwa yakini marudio yao yatakuwa kwenye Jahanamu.

70. Hakika wao waliwakuta baba zao wakipotea.

71. Na wao pia wanaendeshwa kasi katika nyayo zao.

اَفَمَا نَحْنُ بِمَيِّتِيْنَ ﴿٥٩﴾

اِلَّا مَوْتَتَنَا الْاُوْلٰى وَمَا نَحْنُ بِمُعَذَّبِيْنَ ﴿٦٠﴾

اِنَّ هٰذَا لَهُوَ الْفَوْزُ الْعَظِيْمُ ﴿٦١﴾

لِمِثْلِ هٰذَا فَلْيَعْمَلِ الْعٰمِلُوْنَ ﴿٦٢﴾

اَذٰلِكَ خَيْرٌ نُّزُلًا اَمْ شَجَرَةُ الزَّقُّوْمِ ﴿٦٣﴾

اِنَّا جَعَلْنٰهَا فِتْنَةً لِّلظّٰلِمِيْنَ ﴿٦٤﴾

اِنَّهَا شَجَرَةٌ تَخْرُجُ فِيْٓ اَصْلِ الْجَحِيْمِ ﴿٦٥﴾

طَلْعُهَا كَاَنَّهٗ رُءُوْسُ الشَّيٰطِيْنِ ﴿٦٦﴾

فَاِنَّهُمْ لَاٰكِلُوْنَ مِنْهَا فَمَالِـُٔوْنَ مِنْهَا الْبُطُوْنَ ﴿٦٧﴾

ثُمَّ اِنَّ لَهُمْ عَلَيْهَا لَشَوْبًا مِّنْ حَمِيْمٍ ﴿٦٨﴾

ثُمَّ اِنَّ مَرْجِعَهُمْ لَاِلَى الْجَحِيْمِ ﴿٦٩﴾

اِنَّهُمْ اَلْفَوْا اٰبَآءَهُمْ ضَآلِّيْنَ ﴿٧٠﴾

فَهُمْ عَلٰٓى اٰثٰرِهِمْ يُهْرَعُوْنَ ﴿٧١﴾

Aya 63. *Zaqquum.* Baidhawi anaeleza ya kuwa *zaqquum* ni mti mmoja wenye majani madogo, unukao na mchungu, unaopatikana Tihama. Kadhalika chakula cho chote kinachofisha kinaitwa *zaqquum* (Taj, Lane).

Kadhalika neno *zaqquum* ni kifupi cha Aya hii *Dhuq innaka antal aziizul kariim: Dhuq* yaani "Onja" na *uum* ni kifupisho cha sehemu ya Aya iliyobaki. Aya hii nzima tafsiri yake ni hii, *Onja! Hakika wewe ndiye mwenye nguvu, mheshimiwa!* (sura 44:50).

Ni wazi ya kuwa mtu mwenye dhambi asingelazimishwa kuonja matunda haya na masumbufu hayo kama asingejivuna, au kama asingelikataa kweli kwa sababu ya heshima na ukuu wake wa kujisingizia kutupu (Uislmu na Hekima yake).

Aya 66. Waarabu wanamwita *Shaitaan* nyoka fulani mwenye manyoya shingoni, mwenye uso na kichwa kibaya. Pia neno *Shaitaan* ni jina la mti fulani wenye sura mbaya (Taj na Lane).

Kadhalika neno *Shaitaan* maana yake ni "Yeye ambaye mwisho wake ni kuangamia" Limechimbuka katika neno la Shait lenye maana ya "kuangamia." Maana ya maneno haya ni kuwa kuula mti huo humletea mtu laana na maangamizo (Uislamu na Hekima yake).

وَلَقَدْ ضَلَّ قَبْلَهُمْ اَكْثَرُ الْاَوَّلِيْنَ ﴿٧٢﴾

72. Na bila shaka watu wengi wa zamani walipotea kabla yao.

وَلَقَدْ اَرْسَلْنَا فِيْهِمْ مُّنْذِرِيْنَ ﴿٧٣﴾

73. Na hakika Tulipeleka Waonyaji kati yao.

فَانْظُرْ كَيْفَ كَانَ عَاقِبَةُ الْمُنْذَرِيْنَ ﴿٧٤﴾

74. Basi tazama ulikuwaje mwisho wa wale walioonywa?

اِلَّا عِبَادَ اللّٰهِ الْمُخْلَصِيْنَ ﴿٧٥﴾ ع ٢

75. Isipokuwa watumishi wa Allah walioteuliwa.

FUNGU 3

وَلَقَدْ نَادٰىنَا نُوْحٌ فَلَنِعْمَ الْمُجِيْبُوْنَ ﴿٧٦﴾ ۖ

76. Na kwa yakini Nuhu alituita, basi Tu Waitikiaji wema walioje Sisi!

وَنَجَّيْنٰهُ وَاَهْلَهٗ مِنَ الْكَرْبِ الْعَظِيْمِ ﴿٧٧﴾ ۖ

77. Na Tulimwokoa yeye na watu wake katika msiba mkubwa.

وَجَعَلْنَا ذُرِّيَّتَهٗ هُمُ الْبٰقِيْنَ ﴿٧٨﴾ ۗ

78. Na Tuliwajaalia dhuria zake wawe ndio wenye kubaki.

وَتَرَكْنَا عَلَيْهِ فِى الْاٰخِرِيْنَ ﴿٧٩﴾ ۖ

79. Na Tukamwachia (sifa) katika watu wa baadaye.

سَلٰمٌ عَلٰى نُوْحٍ فِى الْعٰلَمِيْنَ ﴿٨٠﴾

80. Amani iwe kwa Nuhu kwa walimwengu wote.

اِنَّا كَذٰلِكَ نَجْزِى الْمُحْسِنِيْنَ ﴿٨١﴾

81. Kwa hakika hivyo ndivyo Tuwalipavyo wafanyao wema.

اِنَّهٗ مِنْ عِبَادِنَا الْمُؤْمِنِيْنَ ﴿٨٢﴾

82. Kwa hakika yeye alikuwa katika watumishi Wetu waaminio.

ثُمَّ اَغْرَقْنَا الْاٰخَرِيْنَ ﴿٨٣﴾

83. Kisha wengine Tukawagharikisha.

وَاِنَّ مِنْ شِيْعَتِهٖ لَاِبْرٰهِيْمَ ﴿٨٤﴾ ۘ ع ٣

84. Na hakika Ibrahimu pia alikuwa katika kundi lake,

اِذْ جَآءَ رَبَّهٗ بِقَلْبٍ سَلِيْمٍ ﴿٨٥﴾

85. Alipomfikia Mola wake kwa moyo wa unyenyekevu.

اِذْ قَالَ لِاَبِيْهِ وَقَوْمِهٖ مَاذَا تَعْبُدُوْنَ ﴿٨٦﴾ ۚ

86. Alipomwambia baba yake na watu wake, Mnaabudu nini?

اَئِفْكًا اٰلِهَةً دُوْنَ اللّٰهِ تُرِيْدُوْنَ ﴿٨٧﴾ ۖ

87. Je mnawataka miungu waongo badala ya Allah?

Aya 78. Watoto wa Nabii Nuhu waliobaki ni Sam, Ham na Yafith. Inasemekana kuwa Sam alikuwa baba wa Waarabu, Ham baba wa Wahabeshi na Yafith baba wa Warumi (Tirmidh).

فَمَا ظَنُّكُمْ بِرَبِّ الْعٰلَمِيْنَ ﴿٨٨﴾

88. Basi ni nini fikira yenu juu ya Mola wa walimwengu?

فَنَظَرَ نَظْرَةً فِي النُّجُوْمِ ﴿٨٩﴾

89. Kisha akazitazama nyota,

فَقَالَ اِنِّيْ سَقِيْمٌ ﴿٩٠﴾

90. Na akasema: hakika mimi nimekirihishwa .

فَتَوَلَّوْا عَنْهُ مُدْبِرِيْنَ ﴿٩١﴾

91. Nao wakamwacha wakampa kisogo.

فَرَاغَ اِلٰٓى اٰلِهَتِهِمْ فَقَالَ اَلَا تَاْكُلُوْنَ ﴿٩٢﴾

92. Basi alikwenda kwa siri kwa miungu yao na akanena: Je, ninyi hamli?

مَا لَكُمْ لَا تَنْطِقُوْنَ ﴿٩٣﴾

93. Mmekuwaje hamsemi?

فَرَاغَ عَلَيْهِمْ ضَرْبًا بِالْيَمِيْنِ ﴿٩٤﴾

94. Kisha akawageukia kuwapiga kwa mkono wa kulia.

فَاَقْبَلُوْٓا اِلَيْهِ يَزِفُّوْنَ ﴿٩٥﴾

95. Basi (watu) wakamwendea upesi.

قَالَ اَتَعْبُدُوْنَ مَا تَنْحِتُوْنَ ﴿٩٦﴾

96. Akasema: Je, mnaviabudu mnavyovichonga?

وَاللّٰهُ خَلَقَكُمْ وَمَا تَعْمَلُوْنَ ﴿٩٧﴾

97. Hali Allah ndiye Aliyewaumbeni ninyi na mnavyovifanya.

قَالُوا ابْنُوْا لَهٗ بُنْيَانًا فَاَلْقُوْهُ فِي الْجَحِيْمِ ﴿٩٨﴾

98. Wakasema: Mjengeeni jengo kisha mtupeni motoni.

فَاَرَادُوْا بِهٖ كَيْدًا فَجَعَلْنٰهُمُ الْاَسْفَلِيْنَ ﴿٩٩﴾

99. Basi walitaka kumfanyia hila, lakini Tukawafanya kuwa wadhalilifu.

وَقَالَ اِنِّيْ ذَاهِبٌ اِلٰى رَبِّيْ سَيَهْدِيْنِ ﴿١٠٠﴾

100. Na (Ibrahimu) akasema: Namkimbilia Mola wangu, punde Ataniongoza.

رَبِّ هَبْ لِيْ مِنَ الصّٰلِحِيْنَ ﴿١٠١﴾

101. Ee Mola wangu! Nipe (mwana) miongoni mwa watenda mema.

فَبَشَّرْنٰهُ بِغُلٰمٍ حَلِيْمٍ ﴿١٠٢﴾

102. Ndipo Tukampa habari njema ya mwana mpole.

Aya 90. *Mimi mgonjwa.* Kuna watu wanaofikiri ya kuwa Nabii Ibrahimu aliposema "Mimi mgonjwa" alisema uwongo. Qur'an inasema, Nabii Ibrahimu alikuwa mkweli kabisa (sura 19:42). Yeye ingawa alikuwa mgonjwa lakini kwa kuwahurumia watu wake alitoka kwenda hubiri, akahubiri hata usiku ukaanza kuingia na nyota zikaanza kutoka, akaona afadhali arudi nyumbani kupumzika, na akawaambia ya kuwa yeye ni mgonjwa.

فَلَمَّا بَلَغَ مَعَهُ السَّعْيَ قَالَ يٰبُنَيَّ اِنِّيْٓ
اَرٰى فِي الْمَنَامِ اَنِّيْٓ اَذْبَحُكَ فَانْظُرْ
مَاذَا تَرٰى ؕ قَالَ يٰٓاَبَتِ افْعَلْ مَا تُؤْمَرُ ۫
سَتَجِدُنِيْٓ اِنْ شَآءَ اللّٰهُ مِنَ الصّٰبِرِيْنَ ﴿۱۰۳﴾

103. Basi alipofikia umri wa kuweza kukimbia na kutembea naye, akamwambia: Ewe mwanangu, hakika nimeona katika ndoto ya kwamba ninakuchinja, basi fikiri waonaje? Akasema: Ee baba yangu! Fanya unayoamriwa, utanikuta inshallah miongoni mwa wanaosubiri.

فَلَمَّآ اَسْلَمَا وَتَلَّهٗ لِلْجَبِيْنِ ﴿۱۰۴﴾

104. Basi wote wawili waliporidhika na akamlaza kifudifudi.

وَنَادَيْنٰهُ اَنْ يّٰٓاِبْرٰهِيْمُ ﴿۱۰۵﴾

105. Mara Tukamwita: Ewe Ibrahimu!

قَدْ صَدَّقْتَ الرُّءْيَا ۚ اِنَّا كَذٰلِكَ نَجْزِي
الْمُحْسِنِيْنَ ﴿۱۰۶﴾

106. Umekwisha isadikisha ndoto. Kwa yakini hivi ndivyo Tuwalipavyo watendao mema.

اِنَّ هٰذَا لَهُوَ الْبَلٰٓؤُا الْمُبِيْنُ ﴿۱۰۷﴾

107. Bila shaka (jambo) hili ni jaribio la bayana.

وَفَدَيْنٰهُ بِذِبْحٍ عَظِيْمٍ ﴿۱۰۸﴾

108. Na Tukamkomboa kwa dhabihu kubwa.

وَتَرَكْنَا عَلَيْهِ فِي الْاٰخِرِيْنَ ﴿۱۰۹﴾

109. Na Tukamwachia sifa kwa watu wa baadaye,

سَلٰمٌ عَلٰٓى اِبْرٰهِيْمَ ﴿۱۱۰﴾

110. Amani iwe kwa Ibrahimu.

كَذٰلِكَ نَجْزِي الْمُحْسِنِيْنَ ﴿۱۱۱﴾

111. Hivi ndivyo Tunavyowalipa watendao wema.

Aya 103. *Ee mwanangu,* yaani Ismail. Tazameni utii wa kijana huyu. Aliposikia ndoto ya baba yake kuwa inamwamrisha amchinje, hakusita wala hakutia shaka, akakubali mara moja na kumwambia baba yake afanye alivyoamriwa.

Aya 104. Tazameni utii wa Nabii Ibrahimu. Hakuwa na mtoto mpaka alipokuwa na umri wa miaka 80. Sasa amepata mtoto aliyekuwa akiomba, lakini alipoambiwa amchinje hakusita. Katika Sham na Bara Hindi kulikuwa na desturi ya kutoa kafara za wanadamu. Hapa Nabii Ibrahimu alipotaka kufanya jambo hili hili ili kufuata alivyoagizwa na ndoto, Allah akamzuia, na kwa njia hii desturi ile ya kuwatoa kafara wanadamu ikawa imekatazwa na Allah. Kama mtu aone katika ndoto anamchinja mtoto wake mradi wake achinje mnyama kwa sadaka, na pia maana yake amtoe wakfu mwanawe kufanya kazi ya dini, kama alivyompeleka Nabii Ibrahimu mwanawe huko Makka na kumtoa wakfu kwa kazi ya dini.

Aya 108. *Dhabihu kubwa.* Kwa ukumbusho wa sadaka ile ya Nabii Ibrahimu, Waislamu wa dunia nzima wanachinja wanyama katika siku za IIdi kubwa (Id-ul-adh'ha).

إِنَّهُ مِنْ عِبَادِنَا الْمُؤْمِنِيْنَ ﴿١١٢﴾

112. Bila shaka yeye alikuwa miongoni mwa watumishi Wetu walioamini.

وَبَشَّرْنٰهُ بِإِسْحٰقَ نَبِيًّا مِّنَ الصّٰلِحِيْنَ ﴿١١٣﴾

113. Tena Tukambashiria (kumzaa) Isihaka, Nabii miongoni mwa watu wema.

وَبٰرَكْنَا عَلَيْهِ وَعَلٰٓى إِسْحٰقَ ۭ وَمِنْ ذُرِّيَّتِهِمَا مُحْسِنٌ وَّ ظَالِمٌ لِّنَفْسِهٖ مُبِيْنٌ ﴿١١٤﴾ ع ٣٩

114. Na Tukambarikia yeye na pia Isihaka; na katika wazao wao yuko atendaye mema na ajidhulumuye nafsi yake waziwazi.

FUNGU 4

وَلَقَدْ مَنَنَّا عَلٰى مُوْسٰى وَهٰرُوْنَ ﴿١١٥﴾

115. Na kwa hakika Tuliwafanyia ihsani Musa na Harun.

وَنَجَّيْنٰهُمَا وَقَوْمَهُمَا مِنَ الْكَرْبِ الْعَظِيْمِ ﴿١١٦﴾

116. Na Tukawaokoa wao na watu wao katika taabu kubwa.

وَنَصَرْنٰهُمْ فَكَانُوْا هُمُ الْغٰلِبِيْنَ ﴿١١٧﴾

117. Na Tukawasaidia, basi wakawa washindi.

وَاٰتَيْنٰهُمَا الْكِتٰبَ الْمُسْتَبِيْنَ ﴿١١٨﴾

118. Nao wawili Tukawapa Kitabu kibainishacho.

وَهَدَيْنٰهُمَا الصِّرَاطَ الْمُسْتَقِيْمَ ﴿١١٩﴾

119. Na Tukawaongoza katika njia iliyonyooka.

وَتَرَكْنَا عَلَيْهِمَا فِي الْاٰخِرِيْنَ ﴿١٢٠﴾

120. Kisha Tukawaachia (sifa) katika watu wa baadaye.

Aya 113. Sasa Nabii Ibrahimu akapewa habari ya kuzaliwa mtoto mwingine aitwaye Isihaka. Hapa ni wazi ya kuwa mtoto aliyetolewa kafara na Nabii Ibrahimu alikuwa Ismail, siye Isihaka kama isemavyo Biblia.

Aya 114. Katika Qur'an Tukufu neno *dhaalimun* (madhalimu) au *dhulmun* (dhulma) halitumiki kila mara kama laana pasipokuwa na tofauti. Linapotumika kwa maana hii linajumuisha aina zote za kujitoa katika njia iliyo sawa. Hata hivyo ziko baadhi ya tofauti ambapo linatumika kuashiria hali ya kustahili sifa njema.

Katika Suuratul Faatir aya ya 33 (35:33) upo ushahidi bayana kwamba Allah Amejumuisha miongoni mwa watumishi Wake wateule watu ambao ni *dhaalimun li nafsihi* yaani wenye kujidhulumu nafsi zao wakati wakifanya juhudi katika njia ya Allah. Katika kundi hilo hilo wale ambao wako katika daraja la juu kwa kulinganishwa na wenzao wametajwa kuwa ni *muqtasid* na *saabiqun bil khairaat* (35:33).

Kadhalika, kujileta katika utendaji wema kwahitaji kiwango fulani cha kuifanyia nafsi yako jefule na ukatili katika hatua za mwanzo za mapambano ya kiroho. Wale wafanyao hivyo kwa ajili ya kumridhisha Allah bila shaka wanastahili kusifiwa kwa wema, hata hivyo wanazungumziwa kuwa ni *dhaalimun linafsihi* (aliyejifanyia ukatili).

سَلٰمٌ عَلٰى مُوْسٰى وَ هٰرُوْنَ ﴿١٢٠﴾

121. Amani kwa Musa na Harun.

اِنَّا كَذٰلِكَ نَجْزِى الْمُحْسِنِيْنَ ﴿١٢١﴾

122. Bila shaka hivi ndivyo Tunavyowalipa wafanyao mema.

اِنَّهُمَا مِنْ عِبَادِنَا الْمُؤْمِنِيْنَ ﴿١٢٢﴾

123. Kwa yakini wao walikuwa miongoni mwa watumishi Wetu waaminio.

وَ اِنَّ اِلْيَاسَ لَمِنَ الْمُرْسَلِيْنَ ﴿١٢٣﴾

124. Na hakika Ilyasa alikuwa miongoni mwa waliotumwa.

اِذْ قَالَ لِقَوْمِهٖۤ اَلَا تَتَّقُوْنَ ﴿١٢٤﴾

125. Alipowaambia watu wake: Je, hamwogopi?

اَتَدْعُوْنَ بَعْلًا وَّ تَذَرُوْنَ اَحْسَنَ الْخَالِقِيْنَ ﴿١٢٥﴾

126. Je mnamwomba Ba'ali na mnamwacha aliye Mbora wa waumbaji-

اللّٰهَ رَبَّكُمْ وَ رَبَّ اٰبَآئِكُمُ الْاَوَّلِيْنَ ﴿١٢٦﴾

127. Allah, Mola wenu na Mola wa baba zenu wa mwanzo?

فَكَذَّبُوْهُ فَاِنَّهُمْ لَمُحْضَرُوْنَ ﴿١٢٧﴾

128. Lakini wakamkadhibisha; basi bila shaka watahudhurishwa (adhabuni).

اِلَّا عِبَادَ اللّٰهِ الْمُخْلَصِيْنَ ﴿١٢٨﴾

129. Isipokuwa watumishi wa Allah walioteuliwa.

وَ تَرَكْنَا عَلَيْهِ فِى الْاٰخِرِيْنَ ﴿١٢٩﴾

130. Na Tumemwachia (sifa) kwa watu wa mwisho.

سَلٰمٌ عَلٰۤى اِلْ يَاسِيْنَ ﴿١٣٠﴾

131. Amani kwa Ilyasa.

اِنَّا كَذٰلِكَ نَجْزِى الْمُحْسِنِيْنَ ﴿١٣١﴾

132. Bila shaka hivi ndivyo Tunavyowalipa wafanyao wema.

اِنَّهٗ مِنْ عِبَادِنَا الْمُؤْمِنِيْنَ ﴿١٣٢﴾

133. Kwa yakini yeye alikuwa miongoni mwa watumishi wetu waaminio.

وَ اِنَّ لُوْطًا لَّمِنَ الْمُرْسَلِيْنَ ﴿١٣٣﴾

134. Na kwa hakika Luti alikuwa miongoni mwa waliotumwa.

Aya 124. Ilyasa ndiye Elia ambaye ni Nabii aliyefika miaka 500 baada ya Nabii Musa. Katika siku zake watu 400 walikuwa wakiabudu sanamu lililoitwa Baal. Watu hao walishindana na Nabii Ilyas huko Jabal Karmal (Palestine). Nabii Ilyasa aliomba dua na washindani wake wakashindwa.

Mayahudi wanasadiki ya kuwa Nabii Ilyasa alipaa mbinguni (2: Wafalme 2:11-12) na angefika mara ya pili kabla ya Masihi Isa mwana wa Mariamu (Malaki 4:4). Alipofika Masihi Mayahudi walimjadili wakimwambia ya kuwa waliambiwa atafika Masihi baada ya kushuka Ilyasa, na maadamu Ilyasa hajashuka basi yeye hawezi kuwa Masihi wa kweli. Nabii Isa aliwaambia kuwa Nabii Yahya ndiye Ilyasa aliyeahidiwa, naye amekwisha fika; na kwa jibu hili akabatilisha ile imani yao ya kusema Ilyasa alipaa mbinguni na atarudi tena (Matt. 11:15-16).

اِذْ نَجَّيْنٰهُ وَاَهْلَهٗۤ اَجْمَعِيْنَ ﴿١٣٥﴾

135. (Kumbukeni) Tulipomwokoa yeye na ahali zake wote,

اِلَّا عَجُوْزًا فِى الْغٰبِرِيْنَ ﴿١٣٦﴾

136. Isipokuwa mwanamke mkongwe katika wale waliobaki nyuma.

ثُمَّ دَمَّرْنَا الْاٰخَرِيْنَ ﴿١٣٧﴾

137. Kisha wengine Tukawaa-ngamiza.

وَاِنَّكُمْ لَتَمُرُّوْنَ عَلَيْهِمْ مُّصْبِحِيْنَ ﴿١٣٨﴾

138. Na kwa yakini ninyi mnawapita asubuhi,

وَبِالَّيْلِ ؕ اَفَلَا تَعْقِلُوْنَ ﴿١٣٩﴾

139. Na usiku (pia); basi je, hamfahamu?

FUNGU 5

وَاِنَّ يُوْنُسَ لَمِنَ الْمُرْسَلِيْنَ ﴿١٤٠﴾

140. Na hakika Yunus alikuwa miongoni mwa waliotumwa.

اِذْ اَبَقَ اِلَى الْفُلْكِ الْمَشْحُوْنِ ﴿١٤١﴾

141. (Kumbukeni) alipoikimbilia jahazi iliyosheheni.

فَسَاهَمَ فَكَانَ مِنَ الْمُدْحَضِيْنَ ﴿١٤٢﴾

142. Na alipiga kura na akawa mwenye kutupwa nje.

فَالْتَقَمَهُ الْحُوْتُ وَهُوَ مُلِيْمٌ ﴿١٤٣﴾

143. Mara samaki alimmeza hali yu mwenye kulaumiwa.

فَلَوْلَاۤ اَنَّهٗ كَانَ مِنَ الْمُسَبِّحِيْنَ ﴿١٤٤﴾

144. Basi isingalikuwa ya kwamba yeye ni miongoni mwa wamtukuzao (Mungu),

لَلَبِثَ فِىْ بَطْنِهٖۤ اِلٰى يَوْمِ يُبْعَثُوْنَ ﴿١٤٥﴾

145. Bila shaka angalikaa tumboni mwake mpaka siku watakayofufuliwa.

فَنَبَذْنٰهُ بِالْعَرَآءِ وَهُوَ سَقِيْمٌ ﴿١٤٦﴾

146. Lakini Tukamtupa ufukoni hali yu mgonjwa.

Aya 141. Si kama alimkimbia Mungu kama wanavyosema watu wengine, maana Yunus alikuwa Nabii wa Mungu asingeweza kumkimbia Mungu wala hakuna mtu anayeweza kumkimbia Mungu.

Nabii Yunus alitumwa kwa watu wa Minawi, waliokuwa wanapata laki moja na elfu ishirini (sura 37:147, Tirmidh). Watu hawa walikadhibisha ujumbe wake. Allah akamwahidi kuwa wataadhibiwa katika muda wa siku arobaini. Nabii Yunus akautoka mji mbele ili adhabu isimkute humo. Wale watu wa Minawi walipoona alama za adhabu wakafanya toba kwa haraka. Kama ilivyo desturi ya Allah hawaadhibu watu wanaotubu na kuomba msamaha. Basi adhabu ikaondolewa na wasiadhibiwe. Nabii Yunus alipojua hawakuadhibiwa akaogopa kurudi kwa sababu ya kuchelea upinzani wao, na hasa kwa vile ni watu wasiojua kanuni za Allah zinazohusiana na ahadi za adhabu.

وَاَنْۢبَتْنَا عَلَيْهِ شَجَرَةً مِّنْ يَّقْطِيْنٍ ﴿١٤٧﴾

147. Na Tukammeeshea mmea wa mung'unya.

وَاَرْسَلْنٰهُ اِلٰى مِائَةِ اَلْفٍ اَوْ يَزِيْدُوْنَ ﴿١٤٨﴾

148. Na Tulimpeleka kwa (watu) laki moja au zaidi.

فَاٰمَنُوْا فَمَتَّعْنٰهُمْ اِلٰى حِيْنٍ ﴿١٤٩﴾

149. Basi waliamini na Tukawafaidisha kwa muda.

فَاسْتَفْتِهِمْ اَلِرَبِّكَ الْبَنَاتُ وَلَهُمُ الْبَنُوْنَ ﴿١٥٠﴾

150. Na uwaulize: Je, kwa Mola wako ni watoto wa kike na kwa wao wenyewe watoto wa kiume?

اَمْ خَلَقْنَا الْمَلٰٓئِكَةَ اِنَاثًا وَّهُمْ شٰهِدُوْنَ ﴿١٥١﴾

151. Je! Tumewaumba Malaika kuwa wanawake nao wakashuhudia?

اَلَآ اِنَّهُمْ مِّنْ اِفْكِهِمْ لَيَقُوْلُوْنَ ﴿١٥٢﴾

152. Tahadhari, kwa yakini ni katika uzushi wao wanaposema,

وَلَدَ اللّٰهُ ۙ وَاِنَّهُمْ لَكٰذِبُوْنَ ﴿١٥٣﴾

153. Allah Amezaa. Na hakika wao bila shaka ni waongo.

اَصْطَفَى الْبَنَاتِ عَلَى الْبَنِيْنَ ﴿١٥٤﴾

154. Je, Amechagua watoto wa kike kuliko wa kiume?

مَا لَكُمْ ۫ كَيْفَ تَحْكُمُوْنَ ﴿١٥٥﴾

155. Mmekuwaje, mnahukumu namna gani?

اَفَلَا تَذَكَّرُوْنَ ﴿١٥٦﴾

156. Je, hamdhukuru?

اَمْ لَكُمْ سُلْطٰنٌ مُّبِيْنٌ ﴿١٥٧﴾

157. Au mmepata dalili iliyo wazi?

فَاْتُوْا بِكِتٰبِكُمْ اِنْ كُنْتُمْ صٰدِقِيْنَ ﴿١٥٨﴾

158. Basi leteni Kitabu chenu kama mnasema kweli.

وَجَعَلُوْا بَيْنَهٗ وَبَيْنَ الْجِنَّةِ نَسَبًا ؕ وَلَقَدْ عَلِمَتِ الْجِنَّةُ اِنَّهُمْ لَمُحْضَرُوْنَ ﴿١٥٩﴾

159. Na wameweka nasaba kati Yake Yeye na majinni na majinni wamekwisha jua hakika wao watahudhurishwa.

سُبْحٰنَ اللّٰهِ عَمَّا يَصِفُوْنَ ﴿١٦٠﴾

160. Allah Yu mbali na sifa wanazompa.

Aya 148. *Au zaidi.* Mtume *s.a.w*. alipoulizwa iliyozidi ilikuwa adadi gani, alijibu, "Elfu ishirini" (Tirmidh).

Aya 150. Kulikuwa na kabila moja liitwalo 'Aamir katika Bara Arabu, na wao walikuwa wakisadiki kuwa Malaika ni binti za Allah.

Aya 159. Hawa 'Aamir walikuwa wanasema Allah alikuwa akiwaoa majinni na watoto aliozaa nao ndio Malaika.

161. Isipokuwa watumishi wa Allah walioteuliwa.

اِلَّا عِبَادَ اللّٰهِ الْمُخْلَصِيْنَ ﴿١٦١﴾

162. Basi bila shaka ninyi na mnaowaabudu,

فَاِنَّكُمْ وَمَا تَعْبُدُوْنَ ﴿١٦٢﴾

163. Ninyi hamuwezi kumpoteza (yeyote) dhidiYake.

مَآ اَنْتُمْ عَلَيْهِ بِفٰتِنِيْنَ ﴿١٦٣﴾

164. Isipokuwa yule aingiaye Motoni.

اِلَّا مَنْ هُوَ صَالِ الْجَحِيْمِ ﴿١٦٤﴾

165. Na (wamesema): Hakuna ye yote miongoni mwetu ila anapo mahali pake hasa.

وَمَا مِنَّآ اِلَّا لَهٗ مَقَامٌ مَّعْلُوْمٌ ﴿١٦٥﴾

166. Na kwa yakini sisi ndio tujipangao safu.

وَّاِنَّا لَنَحْنُ الصَّآفُّوْنَ ﴿١٦٦﴾

167. Na hakika sisi ndio tumtukuzao.

وَاِنَّا لَنَحْنُ الْمُسَبِّحُوْنَ ﴿١٦٧﴾

168. Na (makafiri) walikuwa wakisema.

وَاِنْ كَانُوْا لَيَقُوْلُوْنَ ﴿١٦٨﴾

169. Tungalikuwa na kumbukumbu ya (watu) wa zamani.

لَوْ اَنَّ عِنْدَنَا ذِكْرًا مِّنَ الْاَوَّلِيْنَ ﴿١٦٩﴾

170. Bila shaka Tungalikuwa watumishi wa Allah waliohalisika.

لَكُنَّا عِبَادَ اللّٰهِ الْمُخْلَصِيْنَ ﴿١٧٠﴾

171. Lakini wakamkataa: basi karibuni watajua.

فَكَفَرُوْا بِهٖ فَسَوْفَ يَعْلَمُوْنَ ﴿١٧١﴾

172. Na bila shaka neno letu limekwisha tangulia kwa Watumishi Wetu Waliotumwa.

وَلَقَدْ سَبَقَتْ كَلِمَتُنَا لِعِبَادِنَا الْمُرْسَلِيْنَ ﴿١٧٢﴾

173. Kwa yakini hao ndio watasaidiwa.

اِنَّهُمْ لَهُمُ الْمَنْصُوْرُوْنَ ﴿١٧٣﴾

Aya 161. Yaani Malaika si binti za Allah bali ni watumishi Wake waliohalisika.

Aya 165. Yaani Malaika. Bibi Aisha anasimulia ya kuwa Mtume *s.a.w.* alisema huko mbinguni hakuna mahali po pote ila pana Malaika, amesimama au amesujudu kumwabudu Mungu.

Aya 172. Neno lililokwisha tolewa ni kuwa Mitume wa Allah lazima watashinda.

وَ اِنَّ جُنْدَنَا لَهُمُ الْغٰلِبُوْنَ ﴿۱۷۳﴾

174. Na hakika jeshi letu tu ndilo litashinda.

فَتَوَلَّ عَنْهُمْ حَتّٰى حِيْنٍ ﴿۱۷۴﴾

175. Basi waache kwa muda kidogo.

وَّ اَبْصِرْهُمْ فَسَوْفَ يُبْصِرُوْنَ ﴿۱۷۵﴾

176. Na waonyeshe, nao hivi karibuni wataona.

اَفَبِعَذَابِنَا يَسْتَعْجِلُوْنَ ﴿۱۷۶﴾

177. Je, wanaihimiza adhabu yetu?

فَاِذَا نَزَلَ بِسَاحَتِهِمْ فَسَآءَ صَبَاحُ الْمُنْذَرِيْنَ ﴿۱۷۷﴾

178. Basi adhabu itakaposhuka uwani kwao, ndipo itakuwa asubuhi mbaya kwa wale walioonywa.

وَتَوَلَّ عَنْهُمْ حَتّٰى حِيْنٍ ﴿۱۷۸﴾

179. Na uwaache kwa muda kidogo.

وَّ اَبْصِرْ فَسَوْفَ يُبْصِرُوْنَ ﴿۱۷۹﴾

180. Na uone, nao hivi karibuni wataona.

سُبْحٰنَ رَبِّكَ رَبِّ الْعِزَّةِ عَمَّا يَصِفُوْنَ ﴿۱۸۰﴾

181. Ameepukana Mola wako, Mola Mwenye enzi, na yale wanayomsifu.

وَسَلٰمٌ عَلَى الْمُرْسَلِيْنَ ﴿۱۸۱﴾

182. Na amani iwe juu ya wale waliotumwa.

وَالْحَمْدُ لِلّٰهِ رَبِّ الْعٰلَمِيْنَ ﴿۱۸۲﴾

183. Na sifa zote njema ni za Allah, Mola wa walimwengu.

سُوْرَةُ صٓ مَكِّيَّةٌ وَّ هِيَ مَعَ الْبَسْمَلَةِ تِسْعٌ وَّ ثَمَانُوْنَ اٰيَةً وَّخَمْسَةُ رُكُوْعَاتٍ

38. SURA SAAD

Imeteremshwa Makka

Ina mafungu 5 na Aya 89 pamoja na Bismillahi

بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ ①

1. Kwa jina la Allah, Mwingi wa rehema Mwingi wa ukarimu.

صٓ وَالْقُرْاٰنِ ذِى الذِّكْرِ ۝ ②

2. (Allah) Mkweli. Naapa kwa Qur'an yenye mawaidha.

بَلِ الَّذِيْنَ كَفَرُوْا فِىْ عِزَّةٍ وَّشِقَاقٍ ③

3. Lakini wale waliokufuru wamo katika majivuno na upinzani.

كَمْ اَهْلَكْنَا مِنْ قَبْلِهِمْ مِّنْ قَرْنٍ فَنَادَوْا وَّلَاتَ حِيْنَ مَنَاصٍ ④

4. Tumeviangamiza vizazi vingapi kabla yao, wakapiga mayowe (ya kuomba msaada) lakini wakati wa kuokoka umekwisha pita.

وَعَجِبُوْٓا اَنْ جَآءَهُمْ مُّنْذِرٌ مِّنْهُمْ ۫ وَقَالَ الْكٰفِرُوْنَ هٰذَا سٰحِرٌ كَذَّابٌ ۝ ⑤

5. Na walistaajabu ya kwamba aliwafikia Mwonyaji kutoka miongoni mwao, wakasema makafiri: Huyu ni mchawi, mwongo.

اَجَعَلَ الْاٰلِهَةَ اِلٰهًا وَّاحِدًا ۚ اِنَّ هٰذَا لَشَىْءٌ عُجَابٌ ⑥

6. Je, amewafanya miungu wote kuwa Mungu Mmoja, bila shaka hili hakika ni jambo la ajabu.

وَانْطَلَقَ الْمَلَاُ مِنْهُمْ اَنِ امْشُوْا وَاصْبِرُوْا عَلٰٓى اٰلِهَتِكُمْ ۚ اِنَّ هٰذَا لَشَىْءٌ يُّرَادُ ۝ ⑦

7. Na wakaondoka wakubwa wao wakiwaambia: Nendeni mkadumu na miungu wenu, hakika hili ndilo jambo linalotakiwa.

Sura hii inaitwa *Saad* kwa herufi yake ya mkato iliyoko mwanzo wa Aya ya 2; na inaeleza mateso waliyoyapata Manabii kwa maadui zao. Hata Manabii kama Daudi na Suleimani waliotawala falme zenye nguvu, na kama Ayub aliyekuwa tajiri, pia walitaabishwa, hivyo Mtume *s.a.w.* kadhalika hatakosa kusumbuliwa. Lakini kama lionyeshavyo jina la sura ya kwamba Mwenyezi Mungu ni *Mkweli,* ambaye ametoa habari za kushindwa maadui na kuwa haki itashinda na ahadi yake itatimizwa kama ilivyotimizwa kwa kuwaokoa Mitume waliotangulia. Sura hii ilishuka Makka.

Aya 2. *Saad.* (Mungu) Mkweli" ni herufi ya mkato kwa ajili ya sifa ya Allah Saadiq (Mkweli) (Jamiul Bayan).

Neno *dhikr* (mauidha), pia maana yake ni utukufu na heshima (Taj); hivyo itakuwa maana yake, "Qur'an yenye heshima" au "Qur'an yenye utukufu" na watu watakaofuata mafundisho yake watapata heshima na utukufu, na jambo hili litashuhudia ukweli wa Qur'an.

مَا سَمِعْنَا بِهٰذَا فِي الْمِلَّةِ الْاٰخِرَةِ ۚ اِنْ هٰذَآ اِلَّا اخْتِلَاقٌ ۝٨

8. Hatujawahi kusikia kitu kama hicho hata (kuhusiana na) kaumu yoyote ile itakayokuja. Huu sio ila ni uzushi tu.

ءَاُنْزِلَ عَلَيْهِ الذِّكْرُ مِنْۢ بَيْنِنَا ۭ بَلْ هُمْ فِيْ شَكٍّ مِّنْ ذِكْرِيْ ۚ بَلْ لَّمَّا يَذُوْقُوْا عَذَابِ ۝٩

9. Je, ni yeye tu aliyeteremshiwa mawaidha kati yetu? Lakini hao wanayo shaka juu ya mawaidha Yangu; bali hawajaionja adhabu Yangu.

اَمْ عِنْدَهُمْ خَزَاۗىِٕنُ رَحْمَةِ رَبِّكَ الْعَزِيْزِ الْوَهَّابِ ۝١٠

10. Je, wanazo hazina za rehema za Mola wako aliye Mwenye ushindi kamili, Mpaji?

اَمْ لَهُمْ مُّلْكُ السَّمٰوٰتِ وَالْاَرْضِ وَمَا بَيْنَهُمَا ۡ فَلْيَرْتَقُوْا فِي الْاَسْبَابِ ۝١١

11. Au je, wanao ufalme wa mbingu na ardhi na vilivyomo kati yao? Basi na watumie njia zote.

جُنْدٌ مَّا هُنَالِكَ مَهْزُوْمٌ مِّنَ الْاَحْزَابِ ۝١٢

12. (Hili pia) ni jeshi miongoni mwa makundi litakaloshindiwa hapa.

كَذَّبَتْ قَبْلَهُمْ قَوْمُ نُوْحٍ وَّ عَادٌ وَّفِرْعَوْنُ ذُو الْاَوْتَادِ ۝١٣

13. Walikadhibisha kabla yao watu wa Nuhu na Waadi na Firauni mwenye nguvu.

وَثَمُوْدُ وَقَوْمُ لُوْطٍ وَّ اَصْحٰبُ لْـَٔيْكَةِ ۭ اُولٰۗىِٕكَ الْاَحْزَابُ ۝١٤

14. Na Wathamudi, na watu wa Luti, na wakazi wa Porini - hayo ndiyo makundi (yameyotajwa).

اِنْ كُلٌّ اِلَّا كَذَّبَ الرُّسُلَ فَحَقَّ عِقَابِ ۝١٥

15. Hao wote waliwakadhibisha Mitume, basi adhabu Yangu ikalazimu.

FUNGU 2

وَمَا يَنْظُرُ هٰٓؤُلَاۗءِ اِلَّا صَيْحَةً وَّاحِدَةً مَّا لَهَا مِنْ فَوَاقٍ ۝١٦

16. Na hawa hawangojei ila mlio wenye kutisha usio na taakhira.

وَقَالُوْا رَبَّنَا عَجِّلْ لَّنَا قِطَّنَا قَبْلَ يَوْمِ الْحِسَابِ ۝١٧

17. Na husema: Mola wetu, Ututimizie haraka sehemu yetu kabla ya siku ya Hesabu.

Aya 12. Jambo hili lilitokea katika vita vya Ahzab, lilipokuja jeshi kubwa la makafiri kushambulia Madina lakini likashindwa.

Aya 13. *Dhul-Autaad,* "mwenye majeshi" Neno *autaad* maana yake ni mambo inayopigiliwa ardhini nalo hutumiwa kwa muhawara. Mathalan *autaadul-bilaad* maana yake ni wakubwa wa mji (Lisan). *Dhul-autaad* maana yake ni mwenye majeshi mengi" (Baidhawi), na mara nyingi maana yake linakuwa "mwenye ufalme wenye nguvu" (Kash-shaf).

Aya 16. *Fawaaq,* "taakhira" ni muda ulio baina ya kukama titi moja na titi la pili.

اِصْبِرْ عَلٰى مَا يَقُوْلُوْنَ وَاذْكُرْ عَبْدَنَا دَاوٗدَ ذَا الْاَيْدِ ۚ اِنَّهٗۤ اَوَّابٌ ﴿۱۸﴾

18. Subiri ju ya hayo wayasemayo na umkumbuke Mtumishi Wetu Daudi mwenye nguvu; kwa yakini yeye alikuwa mnyenyekevu sana.

اِنَّا سَخَّرْنَا الْجِبَالَ مَعَهٗ يُسَبِّحْنَ بِالْعَشِيِّ وَالْاِشْرَاقِ ﴿۱۹﴾

19. Hakika sisi Tuliitiisha milima pamoja naye, ikitukuza jioni na asubuhi.

وَالطَّيْرَ مَحْشُوْرَةً ؕ كُلٌّ لَّهٗۤ اَوَّابٌ ﴿۲۰﴾

20. Na (Tuliwatiisha kwake) pia ndege waliokusanywa pamoja. Wote walimnyenyekea Yeye.

وَشَدَدْنَا مُلْكَهٗ وَاٰتَيْنٰهُ الْحِكْمَةَ وَفَصْلَ الْخِطَابِ ﴿۲۱﴾

21. Na Tukautia nguvu ufalme wake na Tukampa hekima na (akili ya) kukata hukumu.

وَهَلْ اَتٰىكَ نَبَؤُا الْخَصْمِ ۘ اِذْ تَسَوَّرُوا الْمِحْرَابَ ﴿۲۲﴾ لا

22. Na je imekuwasilia habari ya wagombanao walipopindukia (ukutani kuingia) chumbani?

وقف لازم

اِذْ دَخَلُوْا عَلٰى دَاوٗدَ فَفَزِعَ مِنْهُمْ ؕ قَالُوْا لَا تَخَفْ ۚ خَصْمٰنِ بَغٰى بَعْضُنَا عَلٰى بَعْضٍ فَاحْكُمْ بَيْنَنَا بِالْحَقِّ وَلَا تُشْطِطْ وَاهْدِنَاۤ اِلٰى سَوَآءِ الصِّرَاطِ ﴿۲۳﴾

23. Walipohudhuria kwa Daudi naye akawaogopa. Wakasema: Usiogope; (sisi ni) wagombanao wawili, mmoja wetu anamdhulumu mwenzake; basi hukumu baina yetu kwa haki wala usiruke mipaka, na utuongoze kwenye njia iliyo sawa.

اِنَّ هٰذَاۤ اَخِيْ ۫ لَهٗ تِسْعٌ وَّ تِسْعُوْنَ نَعْجَةً وَّلِيَ نَعْجَةٌ وَّاحِدَةٌ ۫ فَقَالَ اَكْفِلْنِيْهَا وَعَزَّنِيْ فِي الْخِطَابِ ﴿۲۴﴾

24. Hakika huyu ni ndugu yangu; anao kondoo majike tisini na tisa, nami nina kondoo mmoja tu, lakini anasema, Nipe huyo na ananishinda katika mazungumzo.

Aya 19. Nano *jibaalu* (milima) laweza likaamanisha yale makabila ya milimani yenye nguvu ambayo yalitiishwa na Daudi au laweza pia likamaanisha utajiri wa madini wa milimani ambao ulitumika vizuri sana wakati wake.

Aya 20. Neno *attair* (ndege) lina maana ya watu wenye vipawa vya elimu visivyokuwa vya kawaida ambao hupaa juu kwa kutumia mbawa za mafanikio yao.

Aya 24. Kuna hadithi ya uwongo isemayo kwamba Nabii Daudi alinyang'anya mke wa watu. Wanasema ya kuwa Nabii Daudi alikuwa na wake 99 na akapata kumwona mwanamke

قَالَ لَقَدْ ظَلَمَكَ بِسُؤَالِ نَعْجَتِكَ إِلَىٰ
نِعَاجِهِ ۖ وَإِنَّ كَثِيرًا مِّنَ الْخُلَطَاءِ لَيَبْغِي
بَعْضُهُمْ عَلَىٰ بَعْضٍ إِلَّا الَّذِينَ آمَنُوا
وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ وَقَلِيلٌ مَّا هُمْ ۗ وَظَنَّ
دَاوُودُ أَنَّمَا فَتَنَّاهُ فَاسْتَغْفَرَ رَبَّهُ وَخَرَّ
رَاكِعًا وَأَنَابَ ﴿٢٤﴾ ۩

25. Akasema: Kweli amekudhulumu kwa kukuomba kondoo wako kuongeza katika kondoo zake, na bila shaka wengi wa wanaoshirikiana hudhulumiana wao kwa wao, isipokuwa wale walioamini na kutenda mema na hao ni wachache. Na Daudi akaona ya kwamba Tumemjaribu, akaomba ghofira kwa Mola wake, na akaanguka kunyenyekea na akaelekea.

فَغَفَرْنَا لَهُ ذَٰلِكَ ۖ وَإِنَّ لَهُ عِندَنَا لَزُلْفَىٰ
وَحُسْنَ مَآبٍ ﴿٢٥﴾

26. Na Tukamghofiria hayo, kwa hakika alikuwa mbele yetu mwenye cheo cha kukaribiana na mahali pazuri.

يَا دَاوُودُ إِنَّا جَعَلْنَاكَ خَلِيفَةً فِي الْأَرْضِ
فَاحْكُم بَيْنَ النَّاسِ بِالْحَقِّ وَلَا تَتَّبِعِ
الْهَوَىٰ فَيُضِلَّكَ عَن سَبِيلِ اللَّهِ ۚ إِنَّ
الَّذِينَ يَضِلُّونَ عَن سَبِيلِ اللَّهِ لَهُمْ
عَذَابٌ شَدِيدٌ بِمَا نَسُوا يَوْمَ الْحِسَابِ ﴿٢٦﴾ ع

27. Ewe Daudi, hakika Tumekujaalia kuwa Khalifa ardhini, basi uwahukumu watu kwa haki wala usifuate matamanio yakakupoteza katika njia ya Allah. Kwa yakini wale wanaopotea katika njia ya Allah, wao watapata adhabu kali kwa sababu waliisahau siku ya Hesabu.

---

mzuri, mke wa Uria, akampenda, akataka amwoe, basi akampeleka Uria vitani katika safu ya mbele, akauawa, naye akamwoa mkewe. Watungaji hao wanaendelea kuhadithia ya kwamba Malaika wawili wakamfikia Nabii Daudi kwa sura ya watu na wakatoa mashtaka yao kwa namna ambayo Nabii Daud akumbuke dhambi yake. Fahamuni wazi kabisa kisa hiki ni cha uwongo na kinapinzana na sifa zinazoelezwa na Qur'an juu ya Nabii huyu mtukufu. Habari sahihi ni hizi:-

Maadui wawili wa Nabii Daudi walitaka kumshambulia kwa ghafla. Wakifikiri kuwa amelala au ameghafilika, wakapindukia ukutani kumwingilia chumbani mwake. Wale watu walipoona mpango wao umeharibika. wakatunga kisa cha kuwapa udhuru wa kumfikia katika hali ile isiyo ya kawaida. Qur'an haisemi mahali po pote kuwa watu hawa walikuwa Malaika, bali wameitwa *wagombanao.* Ingawa Nabii Daudi alijua nia yao, lakini kwa subira yake alisikiliza kesi yao ya kubuni ambayo walimtaka awakatie wakati ule ule, naye akampa mmoja wao haki.

Imam Razi anasema: "Karibu wanazuoni wote na wale waliotafuta hakika ya kisa hiki wamesema (Nabii Daudi hakuwa na lawama na) kisa alichotungiwa ni uwongo na hadithi yenye uovu. Na Seyidna Ali aliposikia hadithi hii ya uwongo alisema: Ye yote atakayesimulia hadithi hii ya Daudi kama inavyosimuliwa na watu wanaopiga hadithi nitampiga fimbo mia na sitini, na hii ndiyo adhabu ya watu wanaowasingizia Manabii" (Razi).

Maneno haya *istighfara* (akaomba msamaha) na *ghafarnaa* (Tukamsamehe) yanayotokea katika Aya hii na ifuatayo hayaonyeshi kuwa Nabii Daudi alifanya dhambi, maana kama tulivyokwisha lieleza neno hili, kwa Manabii linakuwa na maana ya kuomba kulindwa; na habari hii inaonyesha ya kuwa maadui wa Nabii Daudi walikwisha jasiri mno juu yake hata wakathubutu kuingia nyumbani mwake kwa nia ya kumdhuru. Aya ya 26 inaeleza waziwazi ya kuwa Nabii Daudi alikuwa mwenye cheo cha kukaribiana na Allah na mahali pazuri.

FUNGU 3

وَمَا خَلَقْنَا السَّمَآءَ وَالْاَرْضَ وَمَا بَيْنَهُمَا بَاطِلًا ؕ ذٰلِكَ ظَنُّ الَّذِيْنَ كَفَرُوْا ۚ فَوَيْلٌ لِّلَّذِيْنَ كَفَرُوْا مِنَ النَّارِ ﴿۲۸﴾

28. Na Hatukuziumba mbingu na ardhi na vilivyomo kati yao bure; hii ndiyo dhana ya wale waliokufuru; basi ni msiba wa Moto kwa wale waliokufuru.

اَمْ نَجْعَلُ الَّذِيْنَ اٰمَنُوْا وَعَمِلُوا الصّٰلِحٰتِ كَالْمُفْسِدِيْنَ فِى الْاَرْضِ ۫ اَمْ نَجْعَلُ الْمُتَّقِيْنَ كَالْفُجَّارِ ﴿۲۹﴾

29. Je! Tuwafanye wale walioamini na kutenda mema kuwa sawa na wafanyao uharibifu ardhini? Au Tuwafanye wacha Mungu kuwa sawa na waovu?

كِتٰبٌ اَنْزَلْنٰهُ اِلَيْكَ مُبٰرَكٌ لِّيَدَّبَّرُوْٓا اٰيٰتِهٖ وَلِيَتَذَكَّرَ اُولُوا الْاَلْبَابِ ﴿۳۰﴾

30. Kitabu adhimu Tumechokiteremsha kwako, chenye baraka ili wapate kuzitafakari Aya zake, na wenye akili washike nasaha.

وَوَهَبْنَا لِدَاوٗدَ سُلَيْمٰنَ ؕ نِعْمَ الْعَبْدُ ؕ اِنَّهٗٓ اَوَّابٌ ﴿۳۱﴾

31. Na Tukampa Daudi, Sulemani, mja mwema aliyoje; bila shaka alikuwa mnyenyekevu mno.

اِذْ عُرِضَ عَلَيْهِ بِالْعَشِيِّ الصّٰفِنٰتُ الْجِيَادُ ۙ﴿۳۲﴾

32. (Kumbukeni) alipopelekewa jioni farasi wa mbegu bora wakimbiao kasi.

فَقَالَ اِنِّٓىْ اَحْبَبْتُ حُبَّ الْخَيْرِ عَنْ ذِكْرِ رَبِّىْ ۚ حَتّٰى تَوَارَتْ بِالْحِجَابِ ﴿۳۳﴾

33. Basi akasema: Navipenda vitu vizuri kwa ajili ya kumkumbuka Mola wangu. Mpaka walipofichika nyuma ya pazia,

رُدُّوْهَا عَلَىَّ ؕ فَطَفِقَ مَسْحًا ۢ بِالسُّوْقِ وَالْاَعْنَاقِ ﴿۳۴﴾

34. (Akasema) Warudisheni kwangu, na akaanza kuwapangusa miguu yao na shingo zao (kwa upendo).

Aya 34. Mafundi wa ngano (hadithi) wameunda nyingine na hapa pia. Wanasema Nabii Sulemani alikuwa akiwatazama farasi hata akasahau Sala ya Alasiri na jua likatua. Nabii Sulemani akasema; Lirudisheni jua, likarudishwa na akasali; kisha akaanza kuwakata farasi mashingo na miguu kwa kuwa wao ndiyo wamemchelewesha!

Maneno ya Qur'an ni haya mbele yetu na hayana kisa cha namna hii. Wala isingempasa Nabii Sulemani kuwaua bure farasi na hali kuchelewa kwake si kosa lao. Wala katika Aya hizi hakuna habari za kuchelewa sala ya Alasiri, wala hakuna habari ya kukata farasi mashingo na miguu. Kwa hakika ni jambo baya sana kuchukua Aya za Allah na kuzitungia visa vya uwongo. Tafsiri iliyo wazi ni hii:-

"Kumbukeni alipopelekewa jioni farasi walio kimya wasimamapo, wepesi wakimbiapo. Akasema: Navipenda vitu vizuri kwa kumkumbuka Mola wangu: hata farasi waliingia zizini. (Akasema) warudisheni kwangu, na akawapangusa miguu yao na shingo zao." Kwa kuwapenda.

Sasa hapa iko wapi Sala ya Alasiri, na jua, na kukata, na kuchelewa, na kadha wa kadha?

35. Na hakika Tulimjaribu Suleimani na Tukauweka mwili (usio na akili wala busara) juu ya kiti chake (cha enzi), kisha akaelekea (kwa Allah).

وَلَقَدْ فَتَنَّا سُلَيْمٰنَ وَاَلْقَيْنَا عَلٰى كُرْسِيِّهٖ جَسَدًا ثُمَّ اَنَابَ ﴿٣٥﴾

36. Akasema: Ee Mola wangu, Unisamehe na Unipe ufalme ambao hataupata ye yote baada yangu. Bila shaka Wewe Ndiwe Mpaji Mkuu.

قَالَ رَبِّ اغْفِرْ لِيْ وَهَبْ لِيْ مُلْكًا لَّا يَنْۢبَغِيْ لِاَحَدٍ مِّنْۢ بَعْدِيْ ۚ اِنَّكَ اَنْتَ الْوَهَّابُ ﴿٣٦﴾

37. Basi Tukamtiishia upepo ukaenda pole pole kwa amri yake anakotaka kuufikisha.

فَسَخَّرْنَا لَهُ الرِّيْحَ تَجْرِيْ بِاَمْرِهٖ رُخَآءً حَيْثُ اَصَابَ ﴿٣٧﴾

38. Pia mashetani, kila ajengaye na azamiliaye mbizi.

وَالشَّيٰطِيْنَ كُلَّ بَنَّآءٍ وَّغَوَّاصٍ ﴿٣٨﴾

39. Na wengine wafungwao minyororoni.

وَّاٰخَرِيْنَ مُقَرَّنِيْنَ فِي الْاَصْفَادِ ﴿٣٩﴾

40. Hiki ndicho Tukitoacho bila ya hesabu, basi fanya ihsani au zuia.

هٰذَا عَطَآؤُنَا فَامْنُنْ اَوْ اَمْسِكْ بِغَيْرِ حِسَابٍ ﴿٤٠﴾

41. Na kwa yakini alikuwa mbele Yetu mwenye cheo cha ukaribu nasi na mwenye makamu mazuri.

وَاِنَّ لَهٗ عِنْدَنَا لَزُلْفٰى وَحُسْنَ مَاٰبٍ ﴿٤١﴾ ع ١٤

FUNGU 4

42. Na umkumbuke Mtumishi Wetu Ayubu alipomwita Mola wake, akinena: Kwa yakini Shetani amenifikishia taabu na adhabu.

وَاذْكُرْ عَبْدَنَآ اَيُّوْبَ ۘ اِذْ نَادٰى رَبَّهٗٓ اَنِّيْ مَسَّنِيَ الشَّيْطٰنُ بِنُصْبٍ وَّعَذَابٍ ﴿٤١﴾

43. Kaza mwendo; hapa (jirani) kuna maji baridi ya kuogea na ya kunywa.

اُرْكُضْ بِرِجْلِكَ ۚ هٰذَا مُغْتَسَلٌۢ بَارِدٌ وَّشَرَابٌ ﴿٤٢﴾

44. Na Tukampa ahali zake na wengine kama wao pamoja nao, kwa rehema itokayo Kwetu na mawaidha kwa watu wenye akili.

وَوَهَبْنَا لَهٗٓ اَهْلَهٗ وَمِثْلَهُمْ مَّعَهُمْ رَحْمَةً مِّنَّا وَذِكْرٰى لِاُولِي الْاَلْبَابِ ﴿٤٣﴾

Aya 35. *Tukaweka mwili juu ya kiti chake,* yaani mtoto wa Nabii Sulemani ambaye alikuwa mwili tu bila akili wala maarifa ya kuwatawala watu. Mahali pengine aneitwa mnyama wa ardhi aliyekula fimbo yake (yaani aliuharibu utawala wa Nabii Sulemani, baba yake) (sura 34:15).

Aya 42. *Shetani* hapa mradi wake ni kiu (Lane, Kamus). Alikuwa katika safari na akapata kiu, basi ndipo akaomba.

45. Na shika kicha cha vijiti mkononi mwako, kisha piga kwacho wala usivunje kiapo, bila shaka Tulimkuta ni mwenye subira, mja mwema kiasi gani! kwa hakika alikuwa mnyenyekevu sana.

وَخُذْ بِيَدِكَ ضِغْثًا فَاضْرِبْ بِّهٖ وَلَا تَحْنَثْ ؕ اِنَّا وَجَدْنٰهُ صَابِرًا ؕ نِعْمَ الْعَبْدُ ؕ اِنَّهٗۤ اَوَّابٌ ﴿۴۴﴾

46. Na uwakumbushe Watumishi Wetu Ibrahimu na Isihaka na Yakubu waliokuwa wenye nguvu na busara.

وَاذْكُرْ عِبٰدَنَاۤ اِبْرٰهِيْمَ وَاِسْحٰقَ وَيَعْقُوْبَ اُولِى الْاَيْدِىْ وَالْاَبْصَارِ ﴿۴۵﴾

47. Hakika Sisi Tuliwachagua hasa kwa ajili ya ukumbusho wa Akhera.

اِنَّاۤ اَخْلَصْنٰهُمْ بِخَالِصَةٍ ذِكْرَى الدَّارِ ﴿۴۶﴾

48. Nao bila shaka walikuwa mbele Yetu miongoni mwa watu bora waliochaguliwa.

وَاِنَّهُمْ عِنْدَنَا لَمِنَ الْمُصْطَفَيْنَ الْاَخْيَارِ ؕ ﴿۴۷﴾

49. Na uwakumbuke Ismaili na Alyasaa na Dhul-Kifli, na hao wote walikuwa miongoni mwa watu bora.

وَاذْكُرْ اِسْمٰعِيْلَ وَالْيَسَعَ وَذَا الْكِفْلِ ؕ وَكُلٌّ مِّنَ الْاَخْيَارِ ؕ ﴿۴۸﴾

50. Huu ni ukumbusho! na kwa yakini wamchao Mungu mahali pao pa kurudia patakuwa pazuri.

هٰذَا ذِكْرٌ ؕ وَاِنَّ لِلْمُتَّقِيْنَ لَحُسْنَ مَاٰبٍ ﴿۴۹﴾ لا

51. Bustani za kukaa milele zilizofunguliwa milango kwa ajili yao.

جَنّٰتِ عَدْنٍ مُّفَتَّحَةً لَّهُمُ الْاَبْوَابُ ﴿۵۰﴾ ج

52. Humo wataegemea matakia na pia humo wataomba matunda mengi na kinywaji.

مُتَّكِـِٕيْنَ فِيْهَا يَدْعُوْنَ فِيْهَا بِفَاكِهَةٍ كَثِيْرَةٍ وَّشَرَابٍ ﴿۵۱﴾

53. Na pamoja nao (watakuwapo) hirimu (zao wenye kulingana umri) wenye macho yenye soni yatazamayo chini.

وَعِنْدَهُمْ قٰصِرٰتُ الطَّرْفِ اَتْرَابٌ ﴿۵۲﴾

54. Haya ndiyo mliyoahidiwa kwa siku ya Hesabu.

هٰذَا مَا تُوْعَدُوْنَ لِيَوْمِ الْحِسَابِ ﴿۵۳﴾ الشافعة

55. Hakika hiyo ndiyo riziki Yetu, haiwezi kumalizika.

اِنَّ هٰذَا لَرِزْقُنَا مَا لَهٗ مِنْ نَّفَادٍ ﴿۵۴﴾ ج

56. Hivyo ndivyo itakavyokuwa, na kwa hakika wale warukao mipaka pa kurudia pao patakuwa pabaya:

هٰذَا ؕ وَاِنَّ لِلطّٰغِيْنَ لَشَرَّ مَاٰبٍ ﴿۵۵﴾ لا

Aya 45. *Shika kicha cha vijiti*, yaani wavute kwako vijana; *piga kwacho,* yaani nenda nao katika kazi ya kuhubiri; *usivunje kiapo,* yaani kiapo cha kukazana katika kazi ya Allah ya kuhubiria watu. Maneno haya *wa laa tahnath* ambayo tumeyafasiri "usivunje kiapo" pia maana yake ni "usielekee batili." (Kamus).

جَهَنَّمَ ۚ يَصْلَوْنَهَا ۚ فَبِئْسَ الْمِهَادُ ﴿٥٧﴾

57. Jahanamu, wataiingia, napo ni mahali pabaya pa kukaa.

هٰذَا ۙ فَلْيَذُوْقُوْهُ حَمِيْمٌ وَّغَسَّاقٌ ﴿٥٨﴾

58. Ndivyo hivyo, basi wayaonje maji yachemkayo na maji yanukayo yenye baridi kali.

وَّاٰخَرُ مِنْ شَكْلِهٖۤ اَزْوَاجٌ ﴿٥٩﴾

59. Na vitakuwepo pia vitu vingine vya namna hii.

هٰذَا فَوْجٌ مُّقْتَحِمٌ مَّعَكُمْ ۚ لَا مَرْحَبًا بِهِمْ ؕ اِنَّهُمْ صَالُوا النَّارِ ﴿٦٠﴾

60. Hili ndilo jeshi litakaloingia pamoja nanyi, hawatapata makaribisho, hakika wao wataingia Motoni.

قَالُوْا بَلْ اَنْتُمْ ۟ لَا مَرْحَبًا بِكُمْ ؕ اَنْتُمْ قَدَّمْتُمُوْهُ لَنَا ۚ فَبِئْسَ الْقَرَارُ ﴿٦١﴾

61. Watasema: Lakini ninyi - nanyi hamna makaribisho! Ninyi ndio mliotutangulizia hii; tena ni kao baya.

قَالُوْا رَبَّنَا مَنْ قَدَّمَ لَنَا هٰذَا فَزِدْهُ عَذَابًا ضِعْفًا فِي النَّارِ ﴿٦٢﴾

62. Watasema: Mola wetu, aliyetutangulizia haya basi mzidishie adhabu mara mbili Motoni.

وَقَالُوْا مَا لَنَا لَا نَرٰى رِجَالًا كُنَّا نَعُدُّهُمْ مِّنَ الْاَشْرَارِ ﴿٦٣﴾

63. Pia watasema: Imekuwaje kwetu, hatuwaoni watu tuliokuwa tukiwahesabu katika waovu?

اَتَّخَذْنٰهُمْ سِخْرِيًّا اَمْ زَاغَتْ عَنْهُمُ الْاَبْصَارُ ﴿٦٤﴾

64. Je, tuliwafanyia mzaha au macho yamewakosa?

اِنَّ ذٰلِكَ لَحَقٌّ تَخَاصُمُ اَهْلِ النَّارِ ﴿٦٥﴾ ع ١٣

65. Bila shaka ni jambo la haki kuhasimiana kwa watu wa Motoni.

FUNGU 5

قُلْ اِنَّمَاۤ اَنَا مُنْذِرٌ ۖ وَّمَا مِنْ اِلٰهٍ اِلَّا اللّٰهُ الْوَاحِدُ الْقَهَّارُ ﴿٦٦﴾ ج

66. Sema: Hakika mimi ni Mwonyaji tu; na hakuna aabudiwaye isipokuwa Allah, Mmoja, Mwenye nguvu.

رَبُّ السَّمٰوٰتِ وَالْاَرْضِ وَمَا بَيْنَهُمَا الْعَزِيْزُ الْغَفَّارُ ﴿٦٧﴾

67. Mola wa mbingu na ardhi na vilivyomo kati yao, Mwenye ushindi kamili, Msamehevu.

قُلْ هُوَ نَبَؤٌا عَظِيْمٌ ﴿٦٨﴾ ۙ

68. Sema: Hii ni habari kuu.

اَنْتُمْ عَنْهُ مُعْرِضُوْنَ ﴿٦٩﴾

69. Mnajiepusha nayo.

مَا كَانَ لِيَ مِنْ عِلْمٍ بِالْمَلَاِ الْاَعْلٰۤى اِذْ يَخْتَصِمُوْنَ ﴿٧٠﴾

70. Sikuwa na elimu yoyote ya wakuu waliotukuka walipokuwa wakijadiliana.

71. Wahyi wafunuliwa kwangu kwamba mimi ni mwonyaji tu dhahiri.

اِنۡ يُّوۡحٰۤى اِلَىَّ اِلَّاۤ اَنَّمَاۤ اَنَا نَذِيۡرٌ مُّبِيۡنٌ ﴿۷۱﴾

72. (Kumbuka) Mola wako Alipowaambia Malaika: Hakika Mimi Nitaumba mtu katika udongo.

اِذۡ قَالَ رَبُّكَ لِلۡمَلٰٓئِكَةِ اِنِّىۡ خَالِقٌۢ بَشَرًا مِّنۡ طِيۡنٍ ﴿۷۲﴾

73. Na Nitakapomkamilisha na kumpulizia roho Yangu, basi angukeni mbele yake mkitii.

فَاِذَا سَوَّيۡتُهٗ وَنَفَخۡتُ فِيۡهِ مِنۡ رُّوۡحِىۡ فَقَعُوۡا لَهٗ سٰجِدِيۡنَ ﴿۷۳﴾

74. Basi Malaika wote wakatii.

فَسَجَدَ الۡمَلٰٓئِكَةُ كُلُّهُمۡ اَجۡمَعُوۡنَ ۙ﴿۷۴﴾

75. Isipokuwa Ibilisi alijivuna naye alikuwa ni miongoni mwa makafiri.

اِلَّاۤ اِبۡلِيۡسَ ؕ اِسۡتَكۡبَرَ وَكَانَ مِنَ الۡكٰفِرِيۡنَ ﴿۷۵﴾

76. Akasema: "Ewe Ibilisi, nini kimekuzuia kukitii kile Nilichokiumba kwa mikono Yangu miwili? Je umefanya kiburi au umekuwa miongoni mwa w--atu wakubwa?

قَالَ يٰۤاِبۡلِيۡسُ مَا مَنَعَكَ اَنۡ تَسۡجُدَ لِمَا خَلَقۡتُ بِيَدَىَّ ؕ اَسۡتَكۡبَرۡتَ اَمۡ كُنۡتَ مِنَ الۡعَالِيۡنَ ﴿۷۶﴾

77. Akasema: Mimi ni bora kuliko yeye; Umeniumba kwa moto naye Umemwumba kwa udongo.

قَالَ اَنَا خَيۡرٌ مِّنۡهُ ؕ خَلَقۡتَنِىۡ مِنۡ نَّارٍ وَّخَلَقۡتَهٗ مِنۡ طِيۡنٍ ﴿۷۷﴾

78. Akasema: Basi toka humo, hakika wewe ndiwe ufukuzwaye.

قَالَ فَاخۡرُجۡ مِنۡهَا فَاِنَّكَ رَجِيۡمٌ ۖ﴿۷۸﴾

79. Na hakika laana Yangu itakuwa juu yako mpaka siku ya Malipo.

وَّاِنَّ عَلَيۡكَ لَعۡنَتِىۡۤ اِلٰى يَوۡمِ الدِّيۡنِ ﴿۷۹﴾

80. Akasema: Mola wangu unipe muhula mpaka siku watakayofufuliwa.

قَالَ رَبِّ فَاَنۡظِرۡنِىۡۤ اِلٰى يَوۡمِ يُبۡعَثُوۡنَ ﴿۸۰﴾

81. Akasema: Haya, hakika u miongoni mwa waliopewa muhula,

قَالَ فَاِنَّكَ مِنَ الۡمُنۡظَرِيۡنَ ۙ﴿۸۱﴾

82. Mpaka wakati wa siku maalumu.

اِلٰى يَوۡمِ الۡوَقۡتِ الۡمَعۡلُوۡمِ ﴿۸۲﴾

83. Akasema: Kwa haki ya utukufu Wako, bila shaka nitawapoteza wote,

قَالَ فَبِعِزَّتِكَ لَاُغۡوِيَنَّهُمۡ اَجۡمَعِيۡنَ ۙ﴿۸۳﴾

84. Isipokuwa watumishi Wako miongoni mwao waliohalisika.

اِلَّا عِبَادَكَ مِنۡهُمُ الۡمُخۡلَصِيۡنَ ﴿۸۴﴾

Aya 73. *Roho Yangu*, yaani Ufunuo au Wahyi (sura 40:16).

قَالَ فَالْحَقُّ ۖ وَالْحَقَّ أَقُولُ ﴿٨٤﴾

85. Akasema: Basi ukweli ndio huu Nami husema ukweli mtupu.

لَأَمْلَأَنَّ جَهَنَّمَ مِنكَ وَمِمَّن تَبِعَكَ مِنْهُمْ أَجْمَعِينَ ﴿٨٥﴾

86. Kwa yakini Nitaijaza Jahanamu kwa wewe na kwa wale wote wenye kukufuata miongoni mwao.

قُلْ مَا أَسْأَلُكُمْ عَلَيْهِ مِنْ أَجْرٍ وَمَا أَنَا مِنَ الْمُتَكَلِّفِينَ ﴿٨٦﴾

87. Sema: Siwaombeni ujira juu ya hayo, wala mimi si katika wale wanao-jikalifisha.

إِنْ هُوَ إِلَّا ذِكْرٌ لِّلْعَالَمِينَ ﴿٨٧﴾

88. Huu siyo ila ni ukumbusho kwa walimwengu.

وَلَتَعْلَمُنَّ نَبَأَهُ بَعْدَ حِينٍ ﴿٨٨﴾ ع ٢٤

89. Na bila shaka mtaujua uhakika wake hivi karibuni.

سُوْرَةُ الزُّمَرِ مَكِّيَّةٌ وَّ هِيَ مَعَ الْبَسْمَلَةِ سِتٌّ وَّ سَبْعُوْنَ اٰيَةً وَّ ثَمَانِيَةُ رُكُوْعَاتٍ

39. SURA AZ-ZUMAR

Imeteremshwa Makka

Ina mafungu 8 na Aya 76 pamoja na Bismillahi

بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ ①

1. Kwa jina la Allah, Mwingi wa rehema, Mwingi wa ukarimu.

تَنْزِيْلُ الْكِتٰبِ مِنَ اللّٰهِ الْعَزِيْزِ الْحَكِيْمِ ②

2. Uteremsho wa Kitabu (hiki) umetoka kwa Allah, Mwenye ushindi kamili, Mwenye hekima.

اِنَّآ اَنْزَلْنَآ اِلَيْكَ الْكِتٰبَ بِالْحَقِّ فَاعْبُدِ اللّٰهَ مُخْلِصًا لَّهُ الدِّيْنَ ③

3. Kwa yakini Sisi Tumekuteremshia Kitabu kwa haki, basi mwabudu Allah, kwa kumhalisishia dini.

اَلَا لِلّٰهِ الدِّيْنُ الْخَالِصُ ؕ وَالَّذِيْنَ اتَّخَذُوْا مِنْ دُوْنِهٖٓ اَوْلِيَآءَ ۘ مَا نَعْبُدُهُمْ اِلَّا لِيُقَرِّبُوْنَآ اِلَى اللّٰهِ زُلْفٰى ؕ اِنَّ اللّٰهَ يَحْكُمُ بَيْنَهُمْ فِيْ مَا هُمْ فِيْهِ يَخْتَلِفُوْنَ ؕ اِنَّ اللّٰهَ لَا يَهْدِيْ مَنْ هُوَ كٰذِبٌ كَفَّارٌ ④

4. Sikilizeni! Dini halisi ndio inayomstahiki Allah; na wale wanaoshika marafiki wengine badala Yake (husema): Sisi hatuwaabudu hawa ila wapate kutufikisha karibu kabisa na Allah. Hakika Allah Atahukumu baina yao katika yale waliyokuwa wakihitilafiana. Bila shaka Allah Hamwongozi aliye mwongo na asiye na shukrani kabisa.

لَوْ اَرَادَ اللّٰهُ اَنْ يَّتَّخِذَ وَلَدًا لَّاصْطَفٰى مِمَّا يَخْلُقُ مَا يَشَآءُ ۙ سُبْحٰنَهٗ ؕ هُوَ اللّٰهُ الْوَاحِدُ الْقَهَّارُ ⑤

5. Kama Allah Angalitaka kupata mtoto bila shaka Angalichagua Amtakaye miongoni mwa Aliowaumba. Lakini Yu mbali na hayo; Yeye ni Allah, Mmoja wa pekee, Mwenye kushinda.

Jina la sura hii, *Vikosi*, linahusu vikosi viwili, waaminio na wasioamini, na sura hii inaeleza utakavyokuwa mwisho wa kila kundi.

Ingawa William Muir na Rodwell wanafikiri sura hii kuwa ilishuka katika majira ya mwisho ya Makka lakini fikira yao hii haina ushahidi wa kutegemewa. Bishara ya kukimbilia Habeshi iliyomo katika Aya ya 11 imekosewa kufahamiwa kwamba inahusu kuhamia Madina, na kosa hili limewafanya hao mabwana kuifahamu sura hii kuwa ni ya baadaye kushuka Makka. Hakuna katika sura hii habari za hila ya maadui ya kumwua Mtume, bali inaeleza tu upinzani aliofanyiwa. Jambo hili linaonyesha ya kuwa sura hii ni katika zile za majira ya mwanzo katika Makka.

خَلَقَ السَّمٰوٰتِ وَالْاَرْضَ بِالْحَقِّ ۚ يُكَوِّرُ
الَّيْلَ عَلَى النَّهَارِ وَيُكَوِّرُ النَّهَارَ عَلَى الَّيْلِ
وَسَخَّرَ الشَّمْسَ وَالْقَمَرَ ؕ كُلٌّ يَّجْرِيْ
لِاَجَلٍ مُّسَمًّى ؕ اَلَا هُوَ الْعَزِيْزُ
الْغَفَّارُ ۝٦

6. Ameumba mbingu na ardhi kwa haki, Huufunika usiku juu ya mchana, na Huufunika mchana juu ya usiku, na Amevitiisha jua na mwezi, vyote huenda kwa muda uliowekwa; jueni kwamba Yeye ni Mwenye ushindi kamili, Msamehevu.

خَلَقَكُمْ مِّنْ نَّفْسٍ وَّاحِدَةٍ ثُمَّ جَعَلَ مِنْهَا
زَوْجَهَا وَاَنْزَلَ لَكُمْ مِّنَ الْاَنْعَامِ ثَمٰنِيَةَ
اَزْوَاجٍ ؕ يَخْلُقُكُمْ فِيْ بُطُوْنِ اُمَّهٰتِكُمْ
خَلْقًا مِّنْۢ بَعْدِ خَلْقٍ فِيْ ظُلُمٰتٍ ثَلٰثٍ ؕ
ذٰلِكُمُ اللّٰهُ رَبُّكُمْ لَهُ الْمُلْكُ ؕ لَاۤ اِلٰهَ اِلَّا
هُوَ ۚ فَاَنّٰى تُصْرَفُوْنَ ۝٧

7. Amewaumbeni katika nafsi moja, kisha Akamfanya mwenziwe katika hiyo, na Akawateremshieni wanyama wanane kwa jozi. Huwaumbeni matumboni mwa mama zenu umbo baada ya umbo katika giza tatu. Huyo Ndiye Allah, Mola wenu, Ufalme ni Wake, hakuna aabudiwaye ila Yeye, basi ninyi mnageuzwa wapi?

اِنْ تَكْفُرُوْا فَاِنَّ اللّٰهَ غَنِيٌّ عَنْكُمْ ۖ وَلَا
يَرْضٰى لِعِبَادِهِ الْكُفْرَ ۚ وَاِنْ تَشْكُرُوْا
يَرْضَهُ لَكُمْ ؕ وَلَا تَزِرُ وَازِرَةٌ وِّزْرَ
اُخْرٰى ؕ ثُمَّ اِلٰى رَبِّكُمْ مَّرْجِعُكُمْ
فَيُنَبِّئُكُمْ بِمَا كُنْتُمْ تَعْمَلُوْنَ ؕ اِنَّهٗ عَلِيْمٌۢ
بِذَاتِ الصُّدُوْرِ ۝٨

8. Mkikufuru, basi Allah hana haja nanyi, wala Haridhii kufuru kwa watumishi Wake; na kama mkishukuru, hayo Atawaridhieni; wala mbebaji hatabeba mzigo wa mwingine; kisha marudio yenu ni kwa Mola wenu, basi Atawaambieni yale mliyokuwa mkifanya. Bila shaka Yeye ni Mjuzi wa yaliyomo vifuani.

وَاِذَا مَسَّ الْاِنْسَانَ ضُرٌّ دَعَا رَبَّهٗ مُنِيْبًا
اِلَيْهِ ثُمَّ اِذَا خَوَّلَهٗ نِعْمَةً مِّنْهُ نَسِيَ مَا كَانَ
يَدْعُوْۤا اِلَيْهِ مِنْ قَبْلُ وَجَعَلَ لِلّٰهِ اَنْدَادًا
لِّيُضِلَّ عَنْ سَبِيْلِهٖ ؕ قُلْ تَمَتَّعْ بِكُفْرِكَ
قَلِيْلًا ۖ اِنَّكَ مِنْ اَصْحٰبِ النَّارِ ۝٩

9. Na taabu inapomfikia mtu humwita Mola wake akielekea Kwake; kisha Akimpa neema kutoka Kwake, husahau yale aliyokuwa akimwitia zamani, na humfanyia Allah washirika ili apoteze (watu) katika njia Yake. Sema: Ujifu rahishe na kufuru yako muda kidogo, hakika wewe ni miongoni mwa watu wa Motoni.

اَمَّنْ هُوَ قَانِتٌ اٰنَآءَ الَّيْلِ سَاجِدًا وَّقَآئِمًا
يَّحْذَرُ الْاٰخِرَةَ وَ يَرْجُوْا رَحْمَةَ رَبِّهٖ ؕ
قُلْ هَلْ يَسْتَوِى الَّذِيْنَ يَعْلَمُوْنَ وَالَّذِيْنَ
لَا يَعْلَمُوْنَ ؕ اِنَّمَا يَتَذَكَّرُ اُولُوا
الْاَلْبَابِ ۝٩ ع

10. Je, afanyaye ibada wakati wa usiku kwa kusujudu na kusimama akiiogopa Akhera na kutarajia rehema za Mola wake (ni sawa na asiyefanya hayo)?. Sema: Je, wanaweza kuwa sawa wale wanaojua na wale wasiojua? ni wenye akili tu ndio washikao mawaidha.

FUNGU 2

قُلْ يٰعِبَادِ الَّذِيْنَ اٰمَنُوا اتَّقُوْا رَبَّكُمْ ؕ
لِلَّذِيْنَ اَحْسَنُوْا فِىْ هٰذِهِ الدُّنْيَا حَسَنَةٌ ؕ
وَاَرْضُ اللّٰهِ وَاسِعَةٌ ؕ اِنَّمَا يُوَفَّى
الصّٰبِرُوْنَ اَجْرَهُمْ بِغَيْرِ حِسَابٍ ۝١١

11. Sema: Enyi watumishi Wangu mlioamini, Mcheni Mola wenu; wale wafanyao wema katika dunia hii watapata wema, na ardhi ya Allah ina wasaa; bila shaka wafanyao subira watapewa ujira wao pasipo hesabu.

قُلْ اِنِّىْٓ اُمِرْتُ اَنْ اَعْبُدَ اللّٰهَ مُخْلِصًا
لَّهُ الدِّيْنَ ۝١٢

12. Sema: Hakika nimeamrishwa nimwabudu Allah kwa kumhalisishia dini.

وَ اُمِرْتُ لِاَنْ اَكُوْنَ اَوَّلَ الْمُسْلِمِيْنَ ۝١٣

13. Na pia nimeamrishwa ya kwamba niwe wa kwanza wa waliojisalimisha.

قُلْ اِنِّىْٓ اَخَافُ اِنْ عَصَيْتُ رَبِّىْ
عَذَابَ يَوْمٍ عَظِيْمٍ ۝١٤

14. Sema: Mimi naogopa adhabu ya siku kubwa kama nikimwasi Mola wangu.

قُلِ اللّٰهَ اَعْبُدُ مُخْلِصًا لَّهٗ دِيْنِىْ ۝١٥

15. Sema: Namwabudu Allah kwa kumhalisishia dini yangu.

فَاعْبُدُوْا مَا شِئْتُمْ مِّنْ دُوْنِهٖ ؕ قُلْ اِنَّ
الْخٰسِرِيْنَ الَّذِيْنَ خَسِرُوْٓا اَنْفُسَهُمْ
وَاَهْلِيْهِمْ يَوْمَ الْقِيٰمَةِ ؕ اَلَا ذٰلِكَ هُوَ
الْخُسْرَانُ الْمُبِيْنُ ۝١٦

16. Basi ninyi abuduni mnachopenda kinyume Chake; sema: Hakika wapatao hasara ni wale waliozihasirisha nafsi zao na ahali zao siku ya Kiyama. Angalieni! hiyo ndiyo hasara iliyo wazi.

لَهُمْ مِّنْ فَوْقِهِمْ ظُلَلٌ مِّنَ النَّارِ وَمِنْ

17. Juu yao kutakuwa na vivuli vya moto na chini yao pia kutakuwa na vivuli vya moto (yaani moto

Aya 11. *Ardhi ya Mungu ina wasaa.* Maneno haya yanaashiria kuhama kwa Waislamu ambako kutawaletea raha.

Aya 17. *Dhulal*. Neno hili maana yake ni "vivuli" na tumelifasiri "vifuniko" kwa kuwa ndiyo mradi wake.

ndilo jambo ambalo kwalo Allah Huwaogopesha watumishi Wake; hivyo basi, Enyi watumishi Wangu! Niogopeni Mimi tu.

تَحْتِهِمْ ظُلَلٌ ؕ ذٰلِكَ يُخَوِّفُ اللّٰهُ بِهٖ عِبَادَهٗ ؕ يٰعِبَادِ فَاتَّقُوْنِ ﴿١٦﴾

18. Na wale wanaojiepusha kufanya ibada ya masanamu, na hunyenyekea kwa Allah, habari njema ni kwao; basi wape habari njema watumishi Wangu:

وَالَّذِيْنَ اجْتَنَبُوا الطَّاغُوْتَ اَنْ يَّعْبُدُوْهَا وَاَنَابُوْٓا اِلَى اللّٰهِ لَهُمُ الْبُشْرٰى ۚ فَبَشِّرْ عِبَادِ ﴿١٧﴾

19. Ambao husikiliza kauli kisha wanafuata wema wake. Hao ndio Aliowaongoza Allah, na hao ndio wenye akili.

الَّذِيْنَ يَسْتَمِعُوْنَ الْقَوْلَ فَيَتَّبِعُوْنَ اَحْسَنَهٗ ؕ اُولٰٓئِكَ الَّذِيْنَ هَدٰىهُمُ اللّٰهُ وَاُولٰٓئِكَ هُمْ اُولُوا الْاَلْبَابِ ﴿١٨﴾

20. Je, iliyemwajibikia kauli ya adhabu: je, unaweza kumwokoa aliyomo katika Moto?

اَفَمَنْ حَقَّ عَلَيْهِ كَلِمَةُ الْعَذَابِ ؕ اَفَاَنْتَ تُنْقِذُ مَنْ فِى النَّارِ ﴿١٩﴾

21. Lakini waliomcha Mola wao watapata ghorofa zilizojengwa juu ya ghorofa, ndani yake hupita mito, ndiyo ahadi ya Allah, Allah Havunji ahadi.

لٰكِنِ الَّذِيْنَ اتَّقَوْا رَبَّهُمْ لَهُمْ غُرَفٌ مِّنْ فَوْقِهَا غُرَفٌ مَّبْنِيَّةٌ ۙ تَجْرِىْ مِنْ تَحْتِهَا الْاَنْهٰرُ ؕ وَعْدَ اللّٰهِ ؕ لَا يُخْلِفُ اللّٰهُ الْمِيْعَادَ ﴿٢٠﴾

22. Je, huoni kwamba Allah Amete remsha maji kutoka mawinguni, kisha Akayaendesha kuwa chemchem ardhini, tena Akaotesha kwayo mimea ya rangi mbalimbali, kisha hunyauka ukaiona inakuwa kimanjano, kisha Huifanya kusagikasagika. Bila shaka katika hayo umo ukumbusho kwa wenye akili.

اَلَمْ تَرَ اَنَّ اللّٰهَ اَنْزَلَ مِنَ السَّمَآءِ مَآءً فَسَلَكَهٗ يَنَابِيْعَ فِى الْاَرْضِ ثُمَّ يُخْرِجُ بِهٖ زَرْعًا مُّخْتَلِفًا اَلْوَانُهٗ ثُمَّ يَهِيْجُ فَتَرٰىهُ مُصْفَرًّا ثُمَّ يَجْعَلُهٗ حُطَامًا ؕ اِنَّ فِىْ ذٰلِكَ لَذِكْرٰى لِاُولِى الْاَلْبَابِ ﴿٢١﴾ ع ٢ ١٦

FUNGU 3

23. Je, mtu ambaye Allah Amemfungulia kifua chake kwa ajili ya Islam, naye huwa na nuru

اَفَمَنْ شَرَحَ اللّٰهُ صَدْرَهٗ لِلْاِسْلَامِ فَهُوَ

Aya 19. Kauli hapa mradi wake ni Kurani, na kufuata *wema wake* mradi wake ni kufuata fundisho lile linalotakikana katika wakati wake.

Aya 23. *Nuru itokayo kwa Mola wake.* Maneno haya yana namna tatu: (1) Mafundisho

عَلٰى نُوْرٍ مِّنْ رَّبِّهٖ ؕ فَوَيْلٌ لِّلْقٰسِيَةِ قُلُوْبُهُمْ مِّنْ ذِكْرِ اللّٰهِ ؕ اُولٰٓئِكَ فِيْ ضَلٰلٍ مُّبِيْنٍ ﴿٢٣﴾

itokayo kwa Mola wake, (ni sawa na mwenye moyo mgumu?) Basi ole kwa wale wenye mioyo migumu katika kumkumbuka Allah, hao wamo katika upotevu dhahiri.

اَللّٰهُ نَزَّلَ اَحْسَنَ الْحَدِيْثِ كِتٰبًا مُّتَشَابِهًا مَّثَانِيَ ۖ تَقْشَعِرُّ مِنْهُ جُلُوْدُ الَّذِيْنَ يَخْشَوْنَ رَبَّهُمْ ۚ ثُمَّ تَلِيْنُ جُلُوْدُهُمْ وَ قُلُوْبُهُمْ اِلٰى ذِكْرِ اللّٰهِ ؕ ذٰلِكَ هُدَى اللّٰهِ يَهْدِيْ بِهٖ مَنْ يَّشَآءُ ؕ وَمَنْ يُّضْلِلِ اللّٰهُ فَمَا لَهٗ مِنْ هَادٍ ﴿٢٤﴾

24. Allah Ameteremsha hadithi bora: kwa sura ya Kitabu chenye maneno yanayopatana (na) yanayokaririwa, husisimka kwayo ngozi za wale wanaomwogopa Mola wao; kisha ngozi zao na mioyo yao hulainika kwa kumkumbuka Mola wao. Huo ndio mwongozo wa Allah, kwa huo Humwongoza Amtakaye, na anayehukumiwa na Allah kupotea, basi hakuna wa kumwongoza.

اَفَمَنْ يَّتَّقِيْ بِوَجْهِهٖ سُوْٓءَ الْعَذَابِ يَوْمَ الْقِيٰمَةِ ؕ وَقِيْلَ لِلظّٰلِمِيْنَ ذُوْقُوْا مَا كُنْتُمْ تَكْسِبُوْنَ ﴿٢٥﴾

25. Je yule ajilindaye uso wake na adhabu mbaya siku ya Kiyama (ni sawa na asiyejilinda?) Na waliodhulumu wataambiwa: Onjeni mliyokuwa mkiyachuma.

كَذَّبَ الَّذِيْنَ مِنْ قَبْلِهِمْ فَاَتٰىهُمُ الْعَذَابُ مِنْ حَيْثُ لَا يَشْعُرُوْنَ ﴿٢٦﴾

26. Waliokuwa kabla yao walikadhibisha basi adhabu ikawafikia kutoka mahali wasipopatambua.

فَاَذَاقَهُمُ اللّٰهُ الْخِزْيَ فِي الْحَيٰوةِ الدُّنْيَا ۚ وَلَعَذَابُ الْاٰخِرَةِ اَكْبَرُ ۘ لَوْ كَانُوْا يَعْلَمُوْنَ ﴿٢٧﴾

27. Basi Allah Akawaonjesha fedheha katika maisha ya dunia, na adhabu ya Akhera ni kubwa zaidi; laiti wangalijua!

وَلَقَدْ ضَرَبْنَا لِلنَّاسِ فِيْ هٰذَا الْقُرْاٰنِ مِنْ كُلِّ مَثَلٍ لَّعَلَّهُمْ يَتَذَكَّرُوْنَ ﴿٢٨﴾

28. Na bila shaka Tumewapigia watu mifano ya kila namna katika hii Kurani ili wapate kushika nasaha.

---

ya Kurani; (2) Mafundisho ya Mtume *s.a.w.* na (3) Nuru ya imani inayomwezesha mtu kupambanuwa sawa na isiyokuwa sawa.

Aya 24. *Kitabu chenye maneno yanayopatana,* ni Kurani. Mafundisho yake yote yanachukuzana na hayapinzani. Sehemu yake moja inaisadikisha sehemu yake nyingine.

قُرْاٰنًا عَرَبِيًّا غَيْرَ ذِيْ عِوَجٍ لَّعَلَّهُمْ يَتَّقُوْنَ ﴿٢٨﴾

29. Kurani adhimu yenye fasaha na bayana isiyo na upotofu wo wote ili wawe wacha Mungu.

ضَرَبَ اللّٰهُ مَثَلًا رَّجُلًا فِيْهِ شُرَكَآءُ مُتَشٰكِسُوْنَ وَرَجُلًا سَلَمًا لِّرَجُلٍ ؕ هَلْ يَسْتَوِيٰنِ مَثَلًا ؕ اَلْحَمْدُ لِلّٰهِ ۚ بَلْ اَكْثَرُهُمْ لَا يَعْلَمُوْنَ ﴿٢٩﴾

30. Allah Amepiga mfano wa mtu mwenye kumilikiwa na watu wengi wanaogombana, na wa mtu mwingine aliyejitupa kwa mtu mmoja tu, je wako sawa katika hali zao? Alhamdu lillahi, bali wengi wao hawajui

اِنَّكَ مَيِّتٌ وَّاِنَّهُمْ مَّيِّتُوْنَ ﴿٣٠﴾

31. Kwa yakini wewe ni mwenye kufa na hakika wao pia ni wenye kufa.

ثُمَّ اِنَّكُمْ يَوْمَ الْقِيٰمَةِ عِنْدَ رَبِّكُمْ تَخْتَصِمُوْنَ ﴿٣١﴾ ع ٢ ١٧

32. Kisha bila shaka mtagombana siku ya Kiyama mbele ya Mola wenu.

FUNGU 4
JUZU 24

فَمَنْ اَظْلَمُ مِمَّنْ كَذَبَ عَلَى اللّٰهِ وَكَذَّبَ بِالصِّدْقِ اِذْ جَآءَهٗ ؕ اَلَيْسَ فِيْ جَهَنَّمَ مَثْوًى لِّلْكٰفِرِيْنَ ﴿٣٢﴾

33. Basi ni nani mdhalimu mkubwa kuliko yule azuaye uwongo juu ya Allah na kuikadhibisha kweli imfikiapo? Je, siyo katika Jahanamu kao la makafiri?

وَالَّذِيْ جَآءَ بِالصِّدْقِ وَصَدَّقَ بِهٖٓ اُولٰٓئِكَ هُمُ الْمُتَّقُوْنَ ﴿٣٣﴾

34. Na aliyeleta ukweli na aliyeusadikisha hao ndio wamchao Allah.

لَهُمْ مَّا يَشَآءُوْنَ عِنْدَ رَبِّهِمْ ؕ ذٰلِكَ جَزٰٓؤُا الْمُحْسِنِيْنَ ﴿٣٤﴾

35. Watapata watakachotaka kwa Mola wao; hayo ni malipo ya watendao mema;

لِيُكَفِّرَ اللّٰهُ عَنْهُمْ اَسْوَاَ الَّذِيْ عَمِلُوْا وَيَجْزِيَهُمْ اَجْرَهُمْ بِاَحْسَنِ الَّذِيْ كَانُوْا يَعْمَلُوْنَ ﴿٣٥﴾

36. Ili Allah Awafutie ubaya waliofanya na kuwalipa ujira wao kwa wema waliokuwa wakiufanya.

Aya 33. Katika Aya hii wadhalimu wakubwa wametajwa kuwa watu wa namna mbili: (1) mtu ambaye anajisingizia kuwa ameonyeshwa njozi au amepewa ufunuo na Allah na hali hakupewa wala hakuonyeshwa cho chote; (2) mtu ambaye haki itokayo kwa Allah inapomfikia anaikadhibisha na kusema Nabii wa Mungu ameleta uwongo.

37. Je, Allah Hamtoshei mtumishi Wake? Na wanaokuogofisha kwa wale walio kinyume Chake; na Aliyehukumiwa na Allah kupotea, basi hana kiongozi.

اَلَيْسَ اللّٰهُ بِكَافٍ عَبْدَهٗ ؕ وَيُخَوِّفُوْنَكَ بِالَّذِيْنَ مِنْ دُوْنِهٖ ؕ وَمَنْ يُّضْلِلِ اللّٰهُ فَمَا لَهٗ مِنْ هَادٍ ۝٣٧

38. Na ambaye Allah Anamwongoza hakuna awezaye kumpoteza; je, Allah si Mwenye ushindi kamili, Mwenye kisasi?

وَمَنْ يَّهْدِ اللّٰهُ فَمَا لَهٗ مِنْ مُّضِلٍّ ؕ اَلَيْسَ اللّٰهُ بِعَزِيْزٍ ذِى انْتِقَامٍ ۝٣٨

39. Na ukiwauliza: Ni nani aliyeziumba mbingu na ardhi? Bila shaka watasema: Allah. Sema: Je, mnawaona wale mnaowaomba kinyume cha Allah, kama Allah Akitaka kunidhuru, je wao wanaweza kuniondolea dhara Yake? Au Akitaka kunirehemu, je, wao wanaweza kuizuia rehema Yake? Sema: Allah Ananitosha, Kwake wanategemea wanaotegemea.

وَلَئِنْ سَاَلْتَهُمْ مَّنْ خَلَقَ السَّمٰوٰتِ وَالْاَرْضَ لَيَقُوْلُنَّ اللّٰهُ ؕ قُلْ اَفَرَءَيْتُمْ مَّا تَدْعُوْنَ مِنْ دُوْنِ اللّٰهِ اِنْ اَرَادَنِىَ اللّٰهُ بِضُرٍّ هَلْ هُنَّ كٰشِفٰتُ ضُرِّهٖۤ اَوْ اَرَادَنِىْ بِرَحْمَةٍ هَلْ هُنَّ مُمْسِكٰتُ رَحْمَتِهٖ ؕ قُلْ حَسْبِىَ اللّٰهُ ؕ عَلَيْهِ يَتَوَكَّلُ الْمُتَوَكِّلُوْنَ ۝٣٩

40. Sema: Enyi watu wangu! Fanyeni (mtakacho) mahali penu, mimi pia nafanya; basi hivi karibuni mtajua,

قُلْ يٰقَوْمِ اعْمَلُوْا عَلٰى مَكَانَتِكُمْ اِنِّىْ عَامِلٌ ۚ فَسَوْفَ تَعْلَمُوْنَ ۙ۝٤٠

41. Ni nani itakayemfikia adhabu ya kumfedhehesha na itakayemshukia adhabu idumuyo.

مَنْ يَّاْتِيْهِ عَذَابٌ يُّخْزِيْهِ وَيَحِلُّ عَلَيْهِ عَذَابٌ مُّقِيْمٌ ۝٤١

42. Kwa yakini Tumekuteremshia Kitabu kwa ajili ya watu kwa haki, basi anayeongoka ni kwa nafsi yake, na anayepotea bila shaka anapotea kwa hasara (ya nafsi) yake; na wewe siye mlinzi wao.

اِنَّاۤ اَنْزَلْنَا عَلَيْكَ الْكِتٰبَ لِلنَّاسِ بِالْحَقِّ ۚ فَمَنِ اهْتَدٰى فَلِنَفْسِهٖ ۚ وَمَنْ ضَلَّ فَاِنَّمَا يَضِلُّ عَلَيْهَا ۚ وَمَاۤ اَنْتَ عَلَيْهِمْ بِوَكِيْلٍ ۝٤٢ ع ٢

Aya 40. Nabii wa Allah anawaambia maadui zake wafanye kila wawezalo kumpinga na wajikusanye hasa na wasaidiane, lakini mwishoni wataona ya kuwa matokeo mema yamekuwa upande wa Mtume wa Mungu, nao wameshindwa.

FUNGU 5

اَللّٰهُ يَتَوَفَّى الْاَنْفُسَ حِيْنَ مَوْتِهَا وَالَّتِيْ لَمْ تَمُتْ فِيْ مَنَامِهَا ۚ فَيُمْسِكُ الَّتِيْ قَضٰى عَلَيْهَا الْمَوْتَ وَيُرْسِلُ الْاُخْرٰٓى اِلٰٓى اَجَلٍ مُّسَمًّى ۭ اِنَّ فِيْ ذٰلِكَ لَاٰيٰتٍ لِّقَوْمٍ يَّتَفَكَّرُوْنَ ﴿٤٢﴾

43. Allah Huzichukua roho za viumbe wakati wa kifo chao; na zile zisizokufa, katika usingizi wao. Basi Huzizuia zile Alizozikidhia mauti na Huzirudisha nyingine mpaka wakati uliowekwa. Bila shaka katika hayo zimo Ishara kwa watu wanaotafakari.

اَمِ اتَّخَذُوْا مِنْ دُوْنِ اللّٰهِ شُفَعَاۗءَ ۭ قُلْ اَوَلَوْ كَانُوْا لَا يَمْلِكُوْنَ شَيْـــًٔا وَّلَا يَعْقِلُوْنَ ﴿٤٣﴾

44. Au wameshika waombezi kinyume cha Allah? Sema: Hata kama hawana mamlaka juu ya kitu cho chote, wala hawana akili?

قُلْ لِّلّٰهِ الشَّفَاعَةُ جَمِيْعًا ۭ لَهٗ مُلْكُ السَّمٰوٰتِ وَالْاَرْضِ ۭ ثُمَّ اِلَيْهِ تُرْجَعُوْنَ ﴿٤٤﴾

45. Sema: Uombezi wote ni kwa Allah; ufalme wa mbingu na ardhi ni Wake, kisha mtarajeshwa Kwake.

وَاِذَا ذُكِرَ اللّٰهُ وَحْدَهُ اشْمَاَزَّتْ قُلُوْبُ الَّذِيْنَ لَا يُؤْمِنُوْنَ بِالْاٰخِرَةِ ۚ وَاِذَا ذُكِرَ الَّذِيْنَ مِنْ دُوْنِهٖٓ اِذَا هُمْ يَسْتَبْشِرُوْنَ ﴿٤٥﴾

46. Na Anapotajwa Allah Peke Yake mioyo ya wale wasioamini Akhera huchukia, na wanapotajwa wale walio kinyume naye, mara wanafurahi.

قُلِ اللّٰهُمَّ فَاطِرَ السَّمٰوٰتِ وَالْاَرْضِ عٰلِمَ الْغَيْبِ وَالشَّهَادَةِ اَنْتَ تَحْكُمُ بَيْنَ عِبَادِكَ فِيْ مَا كَانُوْا فِيْهِ يَخْتَلِفُوْنَ ﴿٤٦﴾

47. Sema: Ee Mola! Mwumba wa mbingu na ardhi, Mjuzi wa yasiyoonekana na yanayoonekana. Wewe Utahukumu baina ya watumishi Wako katika yale waliyokuwa wakihitalifiana.

وَلَوْ اَنَّ لِلَّذِيْنَ ظَلَمُوْا مَا فِي الْاَرْضِ جَمِيْعًا وَّمِثْلَهٗ مَعَهٗ لَافْتَدَوْا بِهٖ مِنْ سُوْۗءِ الْعَذَابِ يَوْمَ الْقِيٰمَةِ ۭ وَبَدَا لَهُمْ مِّنَ اللّٰهِ مَا لَمْ يَكُوْنُوْا يَحْتَسِبُوْنَ ﴿٤٧﴾

48. Na kama wadhalimu wangalikuwa na vyote vinavyopatikana ardhini, na pamoja navyo vingine kama hivyo, bila shaka wangalivitoa kujikomboa katika adhabu mbaya siku ya Kiyama. Na yatawadhihirikia kwa Allah ambayo hawakuwa wakitazamia.

Aya 43. Neno *tawaffi* maana yake ni kufisha; linakuwa na maana ya kulala pale tu linapofuatana na neno *manaam* (usingizi). Linapokuwa halina alama yo yote ya kuonyesha usingizi, linakuwa halina maana nyingine isipokuwa kifo.

Huzizuia zile alizozikidhia mauti. Maneno haya yanaonyesha ya kuwa mtu aliyekwisha kufa harudi tena duniani.

وَبَدَا لَهُمْ سَيِّاٰتُ مَا كَسَبُوْا وَحَاقَ بِهِمْ مَّا كَانُوْا بِهٖ يَسْتَهْزِءُوْنَ ﴿٤٨﴾

49. Na utawadhihirikia ubaya wa yale waliyoyachuma, na yatawazunguka yale waliyokuwa wakiyafanyia mzaha.

فَاِذَا مَسَّ الْاِنْسَانَ ضُرٌّ دَعَانَا ثُمَّ اِذَا خَوَّلْنٰهُ نِعْمَةً مِّنَّا ۙ قَالَ اِنَّمَآ اُوْتِيْتُهٗ عَلٰى عِلْمٍ ؕ بَلْ هِىَ فِتْنَةٌ وَّلٰكِنَّ اَكْثَرَهُمْ لَا يَعْلَمُوْنَ ﴿٤٩﴾

50. Na dhara inapomgusa mwanadamu hutuomba; kisha Tunapompa neema zitokazo Kwetu, husema: Nimezipewa kwa sababu ya ujuzi. Bali hilo ni jaribio, lakini wengi wao hawajui.

قَدْ قَالَهَا الَّذِيْنَ مِنْ قَبْلِهِمْ فَمَآ اَغْنٰى عَنْهُمْ مَّا كَانُوْا يَكْسِبُوْنَ ﴿٥٠﴾

51. Wamekwisha sema haya wale wa kabla yao, lakini hayakuwafaa waliyokuwa wakiyachuma.

فَاَصَابَهُمْ سَيِّاٰتُ مَا كَسَبُوْا ؕ وَالَّذِيْنَ ظَلَمُوْا مِنْ هٰٓؤُلَآءِ سَيُصِيْبُهُمْ سَيِّاٰتُ مَا كَسَبُوْا ۙ وَمَا هُمْ بِمُعْجِزِيْنَ ﴿٥١﴾

52. Basi ukawasibu ubaya wa yale waliyochuma; na wale waliodhulumu miongoni mwa hawa karibuni utawasibu ubaya wa yale waliyochuma, nao si wadhoofishao.

اَوَلَمْ يَعْلَمُوْٓا اَنَّ اللّٰهَ يَبْسُطُ الرِّزْقَ لِمَنْ يَّشَآءُ وَيَقْدِرُ ؕ اِنَّ فِىْ ذٰلِكَ لَاٰيٰتٍ لِّقَوْمٍ يُّؤْمِنُوْنَ ﴿٥٢﴾ ع ١٦

53. Je, wao hawajui ya kwamba Allah Hutoa riziki nyingi kwa yule Amtakaye na hudhikisha? Kwa hakika katika hayo ziko Ishara kwa watu wanaoamini.

FUNGU 6

قُلْ يٰعِبَادِىَ الَّذِيْنَ اَسْرَفُوْا عَلٰٓى اَنْفُسِهِمْ لَا تَقْنَطُوْا مِنْ رَّحْمَةِ اللّٰهِ ؕ اِنَّ اللّٰهَ يَغْفِرُ الذُّنُوْبَ جَمِيْعًا ؕ اِنَّهٗ هُوَ الْغَفُوْرُ الرَّحِيْمُ ﴿٥٣﴾

54. Sema, Enyi watumishi Wangu mliojidhulumu wenyewe, msikate tamaa katika rehema za Allah; bila shaka Allah Husamehe dhambi zote; hakika Yeye ni Msamehevu, Mrehemevu.

وَاَنِيْبُوْٓا اِلٰى رَبِّكُمْ وَاَسْلِمُوْا لَهٗ مِنْ قَبْلِ اَنْ يَّاْتِيَكُمُ الْعَذَابُ ثُمَّ لَا تُنْصَرُوْنَ ﴿٥٤﴾

55. Na nyenyekeeni kwa Mola wenu na jitupeni Kwake kabla ya kuwafikieni adhabu, kisha hamtasaidiwa.

وَاتَّبِعُوْٓا اَحْسَنَ مَآ اُنْزِلَ اِلَيْكُمْ مِّنْ رَّبِّكُمْ مِّنْ قَبْلِ اَنْ يَّاْتِيَكُمُ الْعَذَابُ بَغْتَةً وَّاَنْتُمْ لَا تَشْعُرُوْنَ ﴿٥٥﴾

56. Na fuateni yaliyo bora katika yale yaliyoteremshwa kwenu kutoka kwa Mola wenu kabla ya kuwafikieni adhabu kwa ghafla na hali hamtambui.

Aya 56. *Ahsana,* "Yaliyo bora" mradi ni Kurani; ndicho kitu kilicho bora zaidi kuliko vitu vyote vilivyoteremshwa na Allah kwa ajili ya wanadamu.

57. Isije nafsi ikasema: Ole wangu kwa yale niliyoyapunguza upande wa Allah na kwa hakika nilikuwa tu miongoni mwa wafanyao mzaha.

اَنْ تَقُوْلَ نَفْسٌ يّٰحَسْرَتٰى عَلٰى مَا فَرَّطْتُّ فِيْ جَنْۢبِ اللّٰهِ وَاِنْ كُنْتُ لَمِنَ السّٰخِرِيْنَ ۙ﴿٥٧﴾

58. Au ikasema: Kama Allah Angeniongoza bila shaka ningekuwa miongoni mwa wamchao;

اَوْ تَقُوْلَ لَوْ اَنَّ اللّٰهَ هَدٰىنِيْ لَكُنْتُ مِنَ الْمُتَّقِيْنَ ۙ﴿٥٨﴾

59. Au ikasema iionapo adhabu: Laiti ningerejea ningekuwa miongoni mwa wafanyao mema.

اَوْ تَقُوْلَ حِيْنَ تَرَى الْعَذَابَ لَوْ اَنَّ لِيْ كَرَّةً فَاَكُوْنَ مِنَ الْمُحْسِنِيْنَ ﴿٥٩﴾

60. Naam! Bila shaka zilikufikia Ishara Zangu lakini ukazikadhibisha na ukajivuna na ukawa miongoni mwa makafiri.

بَلٰى قَدْ جَآءَتْكَ اٰيٰتِيْ فَكَذَّبْتَ بِهَا وَاسْتَكْبَرْتَ وَكُنْتَ مِنَ الْكٰفِرِيْنَ ﴿٦٠﴾

61. Na siku ya Kiyama utawaona wale waliomnenea uwongo Allah nyuso zao zimekuwa nyeusi. Je, si katika Jahanamu kao la wale wanaotakabari?

وَيَوْمَ الْقِيٰمَةِ تَرَى الَّذِيْنَ كَذَبُوْا عَلَى اللّٰهِ وُجُوْهُهُمْ مُّسْوَدَّةٌ ؕ اَلَيْسَ فِيْ جَهَنَّمَ مَثْوًى لِّلْمُتَكَبِّرِيْنَ ﴿٦١﴾

62. Allah Atawaokoa wale wamchao Yeye kwa mafanikio, hautawagusa ubaya wala hawatahuzunika.

وَيُنَجِّي اللّٰهُ الَّذِيْنَ اتَّقَوْا بِمَفَازَتِهِمْ ۫ لَا يَمَسُّهُمُ السُّوْٓءُ وَلَا هُمْ يَحْزَنُوْنَ ﴿٦٢﴾

63. Allah ndiye Mwumba wa kila kitu na Yeye ndiye Mlinzi juu ya kila kitu.

اَللّٰهُ خَالِقُ كُلِّ شَيْءٍ ۫ وَّهُوَ عَلٰى كُلِّ شَيْءٍ وَّكِيْلٌ ﴿٦٣﴾

64. Funguo za mbingu na ardhi ni Zake, na wale waliozikataa Aya za Allah hao ndio wenye hasara.

لَهٗ مَقَالِيْدُ السَّمٰوٰتِ وَالْاَرْضِ ؕ وَالَّذِيْنَ كَفَرُوْا بِاٰيٰتِ اللّٰهِ اُولٰٓئِكَ هُمُ الْخٰسِرُوْنَ ﴿٦٤﴾ ع

ع ٦ ١١ ٣

FUNGU 7

قُلْ اَفَغَيْرَ اللّٰهِ تَاْمُرُوْٓنِّيْٓ اَعْبُدُ اَيُّهَا الْجٰهِلُوْنَ ﴿٦٤﴾

65. Sema: Je, mnaniamuru niabudu kinyume cha Allah, enyi wajinga?

وَلَقَدْ اُوْحِيَ اِلَيْكَ وَاِلَى الَّذِيْنَ مِنْ قَبْلِكَ ۚ لَئِنْ اَشْرَكْتَ لَيَحْبَطَنَّ عَمَلُكَ وَلَتَكُوْنَنَّ مِنَ الْخٰسِرِيْنَ ﴿٦٥﴾

66. Na kwa yakini imefunuliwa kwako na kwa wale wa kabla yako: Kama ukishirikisha, bila shaka vitendo vyako vitaharibika na lazima utakuwa miongoni mwa wenye hasara.

بَلِ اللّٰهَ فَاعْبُدْ وَكُنْ مِّنَ الشّٰكِرِيْنَ ﴿٦٦﴾

67. Bali umwabudu Allah tu na uwe miongoni mwa wenye kushukuru.

وَمَا قَدَرُوا اللّٰهَ حَقَّ قَدْرِهٖ ۖ وَالْاَرْضُ جَمِيْعًا قَبْضَتُهٗ يَوْمَ الْقِيٰمَةِ وَالسَّمٰوٰتُ مَطْوِيّٰتٌۢ بِيَمِيْنِهٖ ۭ سُبْحٰنَهٗ وَتَعٰلٰى عَمَّا يُشْرِكُوْنَ ﴿٦٧﴾

68. Na hawakumheshimu Allah heshima impasayo; na siku ya Kiyama ardhi yote itakuwa mkononi mwake na mbingu zitakunjwa katika mkono Wake wa kuume; Ameepukana na upungufu na Yu juu kabisa kuliko yale wamshirikishayo nayo.

وَنُفِخَ فِي الصُّوْرِ فَصَعِقَ مَنْ فِي السَّمٰوٰتِ وَمَنْ فِي الْاَرْضِ اِلَّا مَنْ شَاۗءَ اللّٰهُ ۭ ثُمَّ نُفِخَ فِيْهِ اُخْرٰى فَاِذَا هُمْ قِيَامٌ يَّنْظُرُوْنَ ﴿٦٨﴾

69. Na litapigwa baragumu ndipo watazimia waliomo mbinguni na waliomo ardhini, ila yule Amtakaye Allah. Tena litapigwa mara nyingine, ndipo watasimama wakiangalia.

وَاَشْرَقَتِ الْاَرْضُ بِنُوْرِ رَبِّهَا وَوُضِعَ الْكِتٰبُ وَجِايْۗءَ بِالنَّبِيّٖنَ وَالشُّهَدَاۗءِ وَقُضِيَ بَيْنَهُمْ بِالْحَقِّ وَهُمْ لَا يُظْلَمُوْنَ ﴿٦٩﴾

70. Na ardhi itang'aa kwa nuru ya Mola wake, na kitabu (cha vitendo) kitawekwa na wataletwa Manabii na mashahidi, na itahukumiwa kati yao kwa haki nao hawatadhulumiwa.

وَوُفِّيَتْ كُلُّ نَفْسٍ مَّا عَمِلَتْ وَهُوَ اَعْلَمُ بِمَا يَفْعَلُوْنَ ﴿٧٠﴾ ع ۷

71. Na kila nafsi itapewa sawasawa yale iliyoyafanya, naye Anajua sana wanayoyatenda.

FUNGU 8

وَسِيْقَ الَّذِيْنَ كَفَرُوْٓا اِلٰى جَهَنَّمَ زُمَرًا ؕ
حَتّٰٓى اِذَا جَآءُوْهَا فُتِحَتْ اَبْوَابُهَا
وَقَالَ لَهُمْ خَزَنَتُهَآ اَلَمْ يَاْتِكُمْ رُسُلٌ
مِّنْكُمْ يَتْلُوْنَ عَلَيْكُمْ اٰيٰتِ رَبِّكُمْ
وَيُنْذِرُوْنَكُمْ لِقَآءَ يَوْمِكُمْ هٰذَا ؕ قَالُوْا
بَلٰى وَلٰكِنْ حَقَّتْ كَلِمَةُ الْعَذَابِ عَلَى
الْكٰفِرِيْنَ ۝٧٢

72. Na waliokufuru watapelekwa kwenye Jahanamu makundi makundi, mpaka watakapoifikia itafunguliwa milango yake, na walinzi wake watawaambia: Je! hawakuwafikieni Mitume kutoka miongoni mwenu wakiwasomeeni Aya za Mola wenu na kuwaonyeni mkutano wa siku yenu hii? Watasema: Ndiyo! Lakini limetimia neno la adhabu juu ya makafiri.

قِيْلَ ادْخُلُوْٓا اَبْوَابَ جَهَنَّمَ خٰلِدِيْنَ فِيْهَا ۚ
فَبِئْسَ مَثْوَى الْمُتَكَبِّرِيْنَ ۝٧٣

73. Itasemwa: Ingieni milango ya Jahanamu mkikaa humo; basi ni baya lilioje kao la wanaotakabari!

وَسِيْقَ الَّذِيْنَ اتَّقَوْا رَبَّهُمْ اِلَى الْجَنَّةِ
زُمَرًا ؕ حَتّٰٓى اِذَا جَآءُوْهَا وَفُتِحَتْ
اَبْوَابُهَا وَقَالَ لَهُمْ خَزَنَتُهَا سَلٰمٌ
عَلَيْكُمْ طِبْتُمْ فَادْخُلُوْهَا خٰلِدِيْنَ ۝٧٤

74. Na waliomcha Mola wao watapelekwa Peponi vikundi vikundi, mpaka watakapoifikia na milango yake itafunguliwa, na walinzi wake watawaambia: Amani juu yenu, furahini, basi ingieni humo mkakae.

وَقَالُوا الْحَمْدُ لِلّٰهِ الَّذِيْ صَدَقَنَا وَعْدَهٗ
وَاَوْرَثَنَا الْاَرْضَ نَتَبَوَّاُ مِنَ الْجَنَّةِ حَيْثُ
نَشَآءُ ۚ فَنِعْمَ اَجْرُ الْعٰمِلِيْنَ ۝٧٥

75. Nao watasema: Sifa zote njema ni za Allah Ambaye Ametutimizia ahadi Yake na Ameturithisha ardhi, tunakaa katika Bustani po pote tupendapo; basi ni malipo mazuri yaliyoje kwa watendao (mema)!

وَتَرَى الْمَلٰٓئِكَةَ حَآفِّيْنَ مِنْ حَوْلِ
الْعَرْشِ يُسَبِّحُوْنَ بِحَمْدِ رَبِّهِمْ ۚ وَقُضِيَ
بَيْنَهُمْ بِالْحَقِّ وَقِيْلَ الْحَمْدُ لِلّٰهِ رَبِّ
الْعٰلَمِيْنَ ۝٧٦ ع

76. Na utawaona Malaika wakizunguka pembeni mwa Kiti cha enzi wakimtukuza Mola wao kwa sifa Zake. Na itahukumiwa kati yao kwa haki na itasemwa: Sifa zote njema ni za Allah, mlezi wa viumbe wote.

ع ۝ ع

سُوْرَةُ الْمُؤْمِنِ مَكِّيَّةٌ وَّ هِيَ مَعَ الْبَسْمَلَةِ سِتٌّ وَّ ثَمَانُوْنَ اٰيَةً وَّ تِسْعَةُ رُكُوْعَاتٍ

40. SURA AL-MU'MIN

Imeteremshwa Makka

Ina mafungu 9 na Aya 86 pamoja na Bismillahi.

بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ ①

1. Kwa jina la Allah, Mwingi wa rehema, Mwingi wa ukarimu.

حٰمٓ ②

2. Ahimidiwaye, Atukuzwaye.

تَنْزِيْلُ الْكِتٰبِ مِنَ اللّٰهِ الْعَزِيْزِ الْعَلِيْمِ ③

3. Uteremsho wa Kitabu umetoka kwa Allah, Mwenye ushindi kamili, Mwenye kujua,

غَافِرِ الذَّنْۢبِ وَقَابِلِ التَّوْبِ شَدِيْدِ الْعِقَابِ ذِى الطَّوْلِ ؕ لَآ اِلٰهَ اِلَّا هُوَ ؕ اِلَيْهِ الْمَصِيْرُ ④

4. Aghofiriye dhambi na Apokeaye toba, Mkali wa kuadhibu, Mwenye ukarimu; hakuna aabudiwaye ila Yeye; marejeo ni Kwake.

مَا يُجَادِلُ فِيْٓ اٰيٰتِ اللّٰهِ اِلَّا الَّذِيْنَ كَفَرُوْا فَلَا يَغْرُرْكَ تَقَلُّبُهُمْ فِى الْبِلَادِ ⑤

5. Habishani katika Aya za Allah ila wale waliokufuru; basi usikudanganye utembezi wao mijini.

كَذَّبَتْ قَبْلَهُمْ قَوْمُ نُوْحٍ وَّالْاَحْزَابُ مِنْۢ بَعْدِهِمْ ۖ وَهَمَّتْ كُلُّ اُمَّةٍۢ بِرَسُوْلِهِمْ لِيَاْخُذُوْهُ وَجٰدَلُوْا بِالْبَاطِلِ لِيُدْحِضُوْا بِهِ الْحَقَّ فَاَخَذْتُهُمْ ۖ فَكَيْفَ كَانَ عِقَابِ ⑥

6. Watu wa Nuhu walikadhibisha kabla yao na makundi (mengine) baada yao; na kila taifa liliazimia juu ya Mtume wao ili wamkamate; na walibishana kwa ubatili ili kuipoteza haki, kwa hiyo Nili-wakamata; basi ilikuwaje adhabu Yangu!

Toka sura hii mpaka sura ya 46 ni fungu jingine la sura saba zinazoanza na *Haa Miim* na kwa hivyo zinaitwa *Dhawaati Haamiim*, yaani sura zinazoanza na *Haa Miim.* Zote zinahusiana na majira yale makafiri walipozidi kufanya upinzani na kuteswa Waislamu kulipoanzishwa na baadhi ya Waislamu wakalazimika wakimbie kwenda Habashi. Sura hizi pia zilishuka majira ya mwisho katika Makka.

Aya 2. *Haa Miim,* "Ahimidiwaye, Atukuzwaye" ni herufi za mkato kwa ajili ya sifa za Mwenyezi Mungu *Haa* ni *Hamiid* au *Hayyun* (Asifiwaye au Aliye hai) na *Miim* ni *Majiid* (Atukuzwaye). Kadhalika herufi hizi zinaweza kuwa na maana ya *Ahkamul-Haakimiin* (Mbora wa mahakimu).

Aya 5. *Usikudanganye utembezi wao mijini,* yaani, heshima ya makafiri na fahari zao zisikudanganye kuwadhania kuwa wamenufaika sana au kuwa Mungu yu radhi nao. Watakaposhikwa na Allah, yao yote hayataweza kuwasaidia.

وَكَذٰلِكَ حَقَّتْ كَلِمَتُ رَبِّكَ عَلَى الَّذِيْنَ كَفَرُوْٓا اَنَّهُمْ اَصْحٰبُ النَّارِ ۝٧

7. Na hivyo ndivyo lilivyotimia neno la Mola wako juu ya wale waliokufuru ya kwamba wao ni watu wa Motoni.

اَلَّذِيْنَ يَحْمِلُوْنَ الْعَرْشَ وَمَنْ حَوْلَهٗ يُسَبِّحُوْنَ بِحَمْدِ رَبِّهِمْ وَيُؤْمِنُوْنَ بِهٖ وَيَسْتَغْفِرُوْنَ لِلَّذِيْنَ اٰمَنُوْا ۚ رَبَّنَا وَسِعْتَ كُلَّ شَيْءٍ رَّحْمَةً وَّعِلْمًا فَاغْفِرْ لِلَّذِيْنَ تَابُوْا وَاتَّبَعُوْا سَبِيْلَكَ وَقِهِمْ عَذَابَ الْجَحِيْمِ ۝٨

8. Wale wakinyanyuao Kiti cha enzi, na wale wanaokizunguka, wanatukuza kwa kumsifu Mola wao na wanamwamini na wanawaombea msamaha walioamini: Mola wetu, Umekienea kila kitu kwa rehema na elimu, basi Uwasamehe waliotubu na wakaifuata njia Yako na Uwaepushe na adhabu ya Jahanamu.

رَبَّنَا وَاَدْخِلْهُمْ جَنّٰتِ عَدْنِ ِۨالَّتِيْ وَعَدْتَّهُمْ وَمَنْ صَلَحَ مِنْ اٰبَآئِهِمْ وَاَزْوَاجِهِمْ وَذُرِّيّٰتِهِمْ ۭ اِنَّكَ اَنْتَ الْعَزِيْزُ الْحَكِيْمُ ۝٩

9. Mola wetu! na Uwaingize katika bustani za milele Ulizowaahidi, na pia waliofanya mema miongoni mwa baba zao na wake zao na watoto wao; bila shaka Wewe ndiwe Mwenye nguvu, Mwenye hekima.

وَقِهِمُ السَّيِّاٰتِ ۭ وَمَنْ تَقِ السَّيِّاٰتِ يَوْمَىِٕذٍ فَقَدْ رَحِمْتَهٗ ۭ وَذٰلِكَ هُوَ الْفَوْزُ الْعَظِيْمُ ۝١٠

10. Na Uwaepushe na maovu, naye umwepushaye na maovu siku hiyo, hakika Umemrehemu; na huo ni ufaulu mkubwa.

FUNGU 2

اِنَّ الَّذِيْنَ كَفَرُوْا يُنَادَوْنَ لَمَقْتُ اللّٰهِ اَكْبَرُ مِنْ مَّقْتِكُمْ اَنْفُسَكُمْ اِذْ تُدْعَوْنَ اِلَى الْاِيْمَانِ فَتَكْفُرُوْنَ ۝١١

11. Kwa hakika wale waliokufuru watanadiwa: Bila shaka kukasirika kwa Allah ni kukubwa kuliko mnavyokasirikiana wenyewe. (Kumbukeni) mlipoitwa kwenye imani lakini mkakataa!

قَالُوْا رَبَّنَآ اَمَتَّنَا اثْنَتَيْنِ وَاَحْيَيْتَنَا اثْنَتَيْنِ فَاعْتَرَفْنَا بِذُنُوْبِنَا فَهَلْ اِلٰى خُرُوْجٍ مِّنْ سَبِيْلٍ ۝١٢

12. Watasema: Mola wetu Umetufisha mara mbili na umetuhuisha mara mbili, basi tunakiri dhambi zetu. Basi je, iko njia ya kutoka?

ذٰلِكُمْ بِاَنَّهٗٓ اِذَا دُعِيَ اللّٰهُ وَحْدَهٗ كَفَرْتُمْ ۚ وَاِنْ يُّشْرَكْ بِهٖ تُؤْمِنُوْا ۭ فَالْحُكْمُ لِلّٰهِ الْعَلِيِّ الْكَبِيْرِ ۝١٣

13. Hayo ni kwa sababu alipotangazwa Allah Peke Yake, mlikataa, na Aliposhirikishwa mkaamini.
Basi hukumu ni Kwake Allah Aliye Juu (na) Mkuu.

هُوَ الَّذِیۡ یُرِیۡکُمۡ اٰیٰتِہٖ وَ یُنَزِّلُ لَکُمۡ مِّنَ السَّمَآءِ رِزۡقًا ؕ وَ مَا یَتَذَکَّرُ اِلَّا مَنۡ یُّنِیۡبُ ﴿۱۴﴾

14. Yeye ndiye Anayewaonyesheni Ishara Zake na Huwateremshieni riziki kutoka mbinguni; na hakuna ashikaye nasaha ila anyenyekeaye.

فَادۡعُوا اللّٰہَ مُخۡلِصِیۡنَ لَہُ الدِّیۡنَ وَ لَوۡ کَرِہَ الۡکٰفِرُوۡنَ ﴿۱۵﴾

15. Basi mwombeni Allah, mkijihalisishia utii Kwake tu, ingawa makafiri wachukie.

رَفِیۡعُ الدَّرَجٰتِ ذُو الۡعَرۡشِ ۚ یُلۡقِی الرُّوۡحَ مِنۡ اَمۡرِہٖ عَلٰی مَنۡ یَّشَآءُ مِنۡ عِبَادِہٖ لِیُنۡذِرَ یَوۡمَ التَّلَاقِ ﴿۱۶﴾ۙ

16. Mpandishaji wa vyeo, Mola Aliye na enzi. Hupeleka ufunuo kwa Amri Yake, kwa yule Amtakaye miongoni mwa watumishi Wake, ili Atoe onyo la siku ya kukutana Naye.

یَوۡمَ ہُمۡ بٰرِزُوۡنَ ۚ لَا یَخۡفٰی عَلَی اللّٰہِ مِنۡہُمۡ شَیۡءٌ ؕ لِمَنِ الۡمُلۡکُ الۡیَوۡمَ ؕ لِلّٰہِ الۡوَاحِدِ الۡقَہَّارِ ﴿۱۷﴾

17. Haitafichika habari yao yoyote kwa Allah: Leo ufalme ni wa nani? Ni wa Allah, Aliye Mmoja, (na) mwenye nguvu zote.

اَلۡیَوۡمَ تُجۡزٰی کُلُّ نَفۡسٍۭ بِمَا کَسَبَتۡ ؕ لَا ظُلۡمَ الۡیَوۡمَ ؕ اِنَّ اللّٰہَ سَرِیۡعُ الۡحِسَابِ ﴿۱۸﴾

18. Leo kila mtu atapewa malipo ya yale aliyoyatenda; hakuna dhuluma leo, bila shaka Allah ni Mwepesi wa kuhesabu.

وَ اَنۡذِرۡہُمۡ یَوۡمَ الۡاٰزِفَۃِ اِذِ الۡقُلُوۡبُ لَدَی الۡحَنَاجِرِ کٰظِمِیۡنَ ؕ مَا لِلظّٰلِمِیۡنَ مِنۡ حَمِیۡمٍ وَّ لَا شَفِیۡعٍ یُّطَاعُ ﴿۱۹﴾

19. Na uwaonye siku (ya saa) ikaribiayo mioyo itakapofika kooni kutokana na huzuni na hofu, wadhalimu hawatakuwa na rafiki mpenzi wala mwombezi atiiwaye.

یَعۡلَمُ خَآئِنَۃَ الۡاَعۡیُنِ وَ مَا تُخۡفِی الصُّدُوۡرُ ﴿۲۰﴾

20. Anajua hiyana ya macho na yanayoficha vifua.

وَ اللّٰہُ یَقۡضِیۡ بِالۡحَقِّ ؕ وَ الَّذِیۡنَ یَدۡعُوۡنَ مِنۡ دُوۡنِہٖ لَا یَقۡضُوۡنَ بِشَیۡءٍ ؕ اِنَّ اللّٰہَ ہُوَ السَّمِیۡعُ الۡبَصِیۡرُ ﴿۲۱﴾ ع ۱۷

21. Na Allah Huhukumu kwa haki; lakini wale wanaowaomba kinyume cha Allah hawahukumu cho chote; kwa hakika Allah ni Asikiaye (na) Aonaye.

Aya 16. *Yulqirruuha*, "Hupeleka ufunuo." Hapa ni wazi kabisa kuwa neno *ruuh* maana yake ni *ufunuo*, si roho: kwani kila mtu hupewa roho, lakini hapa *ruuh* imesemwa inapewa Watumishi Wake anaowataka. Kadhalika Baidhawi anasema hapa hapa ya kuwa *Ruuh* ni *Wahyi* yaani ufunuo.

Aya 19. Hapa inabashiriwa adhabu itakayofika katika siku zinazokaribia. Adhabu ya Akhera imekwisha tajwa katika Aya zilizopita.

FUNGU 3

22. Je, hawakusafiri katika nchi wakaona jinsi ulivyokuwa mwisho wa wale waliokuwa kabla yao? Wao walikuwa wenye nguvu zaidi na athari ardhini kuliko hao, lakini Allah Aliwakamata kwa sababu ya makosa yao; wala hapakuwa na wa kuwalinda na Allah.

اَوَلَمۡ يَسِيۡرُوۡا فِى الۡاَرۡضِ فَيَنۡظُرُوۡا كَيۡفَ كَانَ عَاقِبَةُ الَّذِيۡنَ كَانُوۡا مِنۡ قَبۡلِهِمۡ ؕ كَانُوۡا هُمۡ اَشَدَّ مِنۡهُمۡ قُوَّةً وَّاٰثَارًا فِى الۡاَرۡضِ فَاَخَذَهُمُ اللّٰهُ بِذُنُوۡبِهِمۡ ؕ وَمَا كَانَ لَهُمۡ مِّنَ اللّٰهِ مِنۡ وَّاقٍ ﴿۲۲﴾

23. Hayo ni kwa sababu walikuwa wanawafikia Mitume wao kwa Ishara zilizo wazi, lakini wakawakataa, ndipo Allah Akawakamata. Bila shaka Yeye ni Mwenye nguvu, Mkali wa kuadhibu.

ذٰلِكَ بِاَنَّهُمۡ كَانَتۡ تَّاۡتِيۡهِمۡ رُسُلُهُمۡ بِالۡبَيِّنٰتِ فَكَفَرُوۡا فَاَخَذَهُمُ اللّٰهُ ؕ اِنَّهٗ قَوِىٌّ شَدِيۡدُ الۡعِقَابِ ﴿۲۳﴾

24. Na kwa yakini Tulimtuma Musa pamoja na Ishara Zetu na dalili dhahiri.

وَلَقَدۡ اَرۡسَلۡنَا مُوۡسٰى بِاٰيٰتِنَا وَسُلۡطٰنٍ مُّبِيۡنٍ ۙ﴿۲۴﴾

25. Kwa Firauni na Hamana na Karuni, lakini wakasema: (Huyu ni) mchawi, mwongo mkubwa.

اِلٰى فِرۡعَوۡنَ وَهَامٰنَ وَقَارُوۡنَ فَقَالُوۡا سٰحِرٌ كَذَّابٌ ﴿۲۵﴾

26. Basi alipowaletea haki kutoka Kwetu wakasema: Wauweni watoto wa kiume wa wale walioamini pamoja naye na waacheni hai wanawake wao: Na hila ya makafiri haiwi ila katika upotevu.

فَلَمَّا جَآءَهُمۡ بِالۡحَقِّ مِنۡ عِنۡدِنَا قَالُوا اقۡتُلُوۡۤا اَبۡنَآءَ الَّذِيۡنَ اٰمَنُوۡا مَعَهٗ وَاسۡتَحۡيُوۡا نِسَآءَهُمۡ ؕ وَمَا كَيۡدُ الۡكٰفِرِيۡنَ اِلَّا فِىۡ ضَلٰلٍ ﴿۲۶﴾

27. Na akasema Firauni: Niacheni nimwue Musa, naye amwite Mola wake! Hakika nachelea isije akaibadilisha dini yenu au ataleta matata katika nchi.

وَقَالَ فِرۡعَوۡنُ ذَرُوۡنِىۡۤ اَقۡتُلۡ مُوۡسٰى وَلۡيَدۡعُ رَبَّهٗ ۚ اِنِّىۡۤ اَخَافُ اَنۡ يُّبَدِّلَ دِيۡنَكُمۡ اَوۡ اَنۡ يُّظۡهِرَ فِى الۡاَرۡضِ الۡفَسَادَ ﴿۲۷﴾

28. na Musa akasema: Hakika najikinga kwa Mola wangu na Mola

Aya 22. *Athari.* Neno hili maana yake ni "alama" na "ukumbusho," lakini hapa mradi wake ni ngome na majengo makubwa makubwa (Bayan na Baidhawi). Yaani hao watu wa zamani waliokuwa na nguvu zaidi kuliko ninyi hawakuweza kuwashinda Manabii wa Allah, je mtashinda ninyi?

Aya 28. Jambo la salama kwa mtu ni ya kuwa awe daima katika ulinzi wa Allah, na namna hii ndiyo mtu anaweza kusalimika na taabu na fitina za kila aina.

مِّنْ كُلِّ مُتَكَبِّرٍ لَّا يُؤْمِنُ بِيَوْمِ الْحِسَابِ ﴿٢٧﴾

wenu Anilinde na kila mwenye kiburi, asiyeamini siku ya Hesabu.

FUNGU 4

وَقَالَ رَجُلٌ مُّؤْمِنٌ مِّنْ اٰلِ فِرْعَوْنَ يَكْتُمُ اِيْمَانَهٗۤ اَتَقْتُلُوْنَ رَجُلًا اَنْ يَّقُوْلَ رَبِّيَ اللّٰهُ وَقَدْ جَآءَكُمْ بِالْبَيِّنٰتِ مِنْ رَّبِّكُمْ ؕ وَاِنْ يَّكُ كَاذِبًا فَعَلَيْهِ كَذِبُهٗ ۚ وَاِنْ يَّكُ صَادِقًا يُّصِبْكُمْ بَعْضُ الَّذِيْ يَعِدُكُمْ ؕ اِنَّ اللّٰهَ لَا يَهْدِيْ مَنْ هُوَ مُسْرِفٌ كَذَّابٌ ﴿٢٨﴾

29. Na akasema mtu mumini aliyekuwa mmoja wa watu wa Firauni afichaye imani yake: Je, mtamwua mtu kwa sababu anasema Mola wangu ni Allah? Na kwa yakini yeye amewafikieni kwa dalili wazi zitokazo kwa Mola wenu, naye akiwa mwongo, basi uwongo wake ni juu yake, na kama akiwa mkweli, yatawafikieni baadhi ya hayo anayowaahidini. Bila shaka Allah Hamwongozi yule apitaye kiasi, mwongo mkubwa.

يٰقَوْمِ لَكُمُ الْمُلْكُ الْيَوْمَ ظٰهِرِيْنَ فِي الْاَرْضِ ۫ فَمَنْ يَّنْصُرُنَا مِنْۢ بَاْسِ اللّٰهِ اِنْ جَآءَنَا ؕ قَالَ فِرْعَوْنُ مَاۤ اُرِيْكُمْ اِلَّا مَاۤ اَرٰى وَمَاۤ اَهْدِيْكُمْ اِلَّا سَبِيْلَ الرَّشَادِ ﴿٢٩﴾

30. Enyi watu wangu! Leo ufalme ni wenu, mmeshinda katika ardhi; basi ni nani atakayetusaidia katika adhabu ya Allah kama ikitufikia? Firauni akasema: Sikuwaonyesheni ila niliyoyaona wala siwaongozeni ila kwenye njia ya uongofu.

وَقَالَ الَّذِيْۤ اٰمَنَ يٰقَوْمِ اِنِّيْۤ اَخَافُ عَلَيْكُمْ مِّثْلَ يَوْمِ الْاَحْزَابِ ﴿٣٠﴾ۙ

31. Na yule aliyeamini akasema: Enyi watu wangu! hakika mimi nawahofieni mfano wa siku ya makundi:

مِثْلَ دَاْبِ قَوْمِ نُوْحٍ وَّ عَادٍ وَّ ثَمُوْدَ وَالَّذِيْنَ مِنْۢ بَعْدِهِمْ ؕ وَمَا اللّٰهُ يُرِيْدُ ظُلْمًا لِّلْعِبَادِ ﴿٣١﴾

32. Mfano wa hali ya watu wa Nuhu na 'Ad na Thamud na wale waliokuwa nyuma yao; na Allah Hataki dhuluma kwa watu.

وَيٰقَوْمِ اِنِّيْۤ اَخَافُ عَلَيْكُمْ يَوْمَ التَّنَادِ ﴿٣٢﴾ۙ

33. Na Enyi watu wangu, nawahofieni siku ya kuitana kwa sauti kuu.

يَوْمَ تُوَلُّوْنَ مُدْبِرِيْنَ ۚ مَا لَكُمْ مِّنَ اللّٰهِ مِنْ عَاصِمٍ ۚ وَمَنْ يُّضْلِلِ اللّٰهُ فَمَا لَهٗ مِنْ هَادٍ ﴿٣٣﴾

34. Siku mtakapogeuka kurudi nyuma: hamtakuwa na kuwaokoeni na Allah. Na ahukumiwaye na Allah kupotea, basi huyo hana mwongozi ye yote.

Aya 33. *Siku ya kuitana,* ni siku ya adhabu hapa duniani au Akhera, ambayo watu wakaitana lakini watasambaana ovyo kwa dhiki ya adhabu na hakuna atakayeweza kumsaidia

35. Na bila shaka zamani aliwafikieni Yusuf kwa dalili zilizo wazi, lakini ninyi mliendelea katika shaka kwa yale aliyowaleteeni; mpaka alipofariki mkasema: Allah Hataleta kabisa Mtume baada yake. Kama hivyo Allah Huthibitisha upotevu wa yule aliyepita kiasi, mwenye shaka,

وَلَقَدْ جَآءَكُمْ يُوْسُفُ مِنْ قَبْلُ بِالْبَيِّنٰتِ فَمَا زِلْتُمْ فِيْ شَكٍّ مِّمَّا جَآءَكُمْ بِهٖ ؕ حَتّٰۤى اِذَا هَلَكَ قُلْتُمْ لَنْ يَّبْعَثَ اللّٰهُ مِنْۢ بَعْدِهٖ رَسُوْلًا ؕ كَذٰلِكَ يُضِلُّ اللّٰهُ مَنْ هُوَ مُسْرِفٌ مُّرْتَابُ ۖ﴿۳۴﴾

36. Ambao wanajadiliana katika Ishara za Allah pasipo dalili yo yote iliyowafikia: ni chukizo kubwa mbele ya Allah na mbele ya wale walioamini, hivi ndivyo Apigavyo muhuri juu ya kila moyo wa mjeuri, ajitukuzaye.

الَّذِيْنَ يُجَادِلُوْنَ فِيْۤ اٰيٰتِ اللّٰهِ بِغَيْرِ سُلْطٰنٍ اَتٰىهُمْ ؕ كَبُرَ مَقْتًا عِنْدَ اللّٰهِ وَعِنْدَ الَّذِيْنَ اٰمَنُوْا ؕ كَذٰلِكَ يَطْبَعُ اللّٰهُ عَلٰى كُلِّ قَلْبِ مُتَكَبِّرٍ جَبَّارٍ ﴿۳۵﴾

37. Na Firauni akasema: Ewe Hamana! Nijengee Kasri ili nipate kuzifikia njia.

وَقَالَ فِرْعَوْنُ يٰهَامٰنُ ابْنِ لِيْ صَرْحًا لَّعَلِّيْۤ اَبْلُغُ الْاَسْبَابَ ﴿۳۶﴾

38. Njia za mbinguni ili nimwone Mungu wa Musa; na kwa yakini ninamjua kuwa ni mwongo tu. Na hivi ndivyo Firauni akapambiwa ubaya wa vitendo vyake na akazuiliwa njia (ya haki); lakini hila ya Firauni haikuwa ila katika kuangamia.

اَسْبَابَ السَّمٰوٰتِ فَاَطَّلِعَ اِلٰۤى اِلٰهِ مُوْسٰى وَ اِنِّيْ لَاَظُنُّهٗ كَاذِبًا ؕ وَكَذٰلِكَ زُيِّنَ لِفِرْعَوْنَ سُوْٓءُ عَمَلِهٖ وَصُدَّ عَنِ السَّبِيْلِ ؕ وَ مَا كَيْدُ فِرْعَوْنَ اِلَّا فِيْ تَبَابٍ ﴿۳۷﴾

FUNGU 5

39. Na yule aliyeamini alisema: Enyi watu wangu, nifuateni, nitawaongozeni njia ya uongofu.

وَقَالَ الَّذِيْۤ اٰمَنَ يٰقَوْمِ اتَّبِعُوْنِ اَهْدِكُمْ سَبِيْلَ الرَّشَادِ ﴿۳۸﴾

Aya 35. *Allah Hataleta kabisa Mtume baada yake.* Fikira za namna hii si mpya kwa watu. Toka zamani watu walikuwa wanadhani Nabii fulani ni wa mwisho, na hatakuja Nabii tena baada yake. Lakini Allah anavunja itikadi yao kwa kumtuma Nabii mwingine.

Aya 37-38. Maneno haya Firauni anayasema kwa kejeli.

40. Enyi watu wangu! kwa hakika maisha ya dunia hii ni starehe (ipitayo tu), na bila shaka Akhera ndiyo nyumba ya kukaa.

يٰقَوْمِ اِنَّمَا هٰذِهِ الْحَيٰوةُ الدُّنْيَا مَتَاعٌ ۫ وَّاِنَّ الْاٰخِرَةَ هِيَ دَارُ الْقَرَارِ ﴿٣٩﴾

41. Afanyaye ubaya hatalipwa ila sawa na huo, na afanyaye wema, akiwa mwanamume au mwanamke, naye yu mumini, basi hao wataingia Peponi, wataruzukiwa humo bila hesabu.

مَنْ عَمِلَ سَيِّئَةً فَلَا يُجْزٰٓى اِلَّا مِثْلَهَا ۚ وَمَنْ عَمِلَ صَالِحًا مِّنْ ذَكَرٍ اَوْ اُنْثٰى وَهُوَ مُؤْمِنٌ فَاُولٰٓئِكَ يَدْخُلُوْنَ الْجَنَّةَ يُرْزَقُوْنَ فِيْهَا بِغَيْرِ حِسَابٍ ﴿٤٠﴾

42. Na enyi watu wangu! mimi nina nini, nawaiteni kwenye wokovu nanyi mwaniita kwenye Moto!

وَيٰقَوْمِ مَا لِيْٓ اَدْعُوْكُمْ اِلَى النَّجٰوةِ وَتَدْعُوْنَنِيْٓ اِلَى النَّارِ ﴿٤١﴾

43. Mnaniita nimkufuru Allah na kumshirikisha na yule ambaye simjui, nami nawaiteni kwa Mwenye nguvu, Msamehevu.

تَدْعُوْنَنِيْ لِاَكْفُرَ بِاللّٰهِ وَاُشْرِكَ بِهٖ مَا لَيْسَ لِيْ بِهٖ عِلْمٌ ۫ وَّاَنَا اَدْعُوْكُمْ اِلَى الْعَزِيْزِ الْغَفَّارِ ﴿٤٢﴾

44. Bila shaka ninyi mnaniita kwa yule ambaye hana wito duniani wala Akhera, na marudio yetu ni kwa Allah, na wapitao kiasi hao ndio watu wa Motoni.

لَا جَرَمَ اَنَّمَا تَدْعُوْنَنِيْٓ اِلَيْهِ لَيْسَ لَهٗ دَعْوَةٌ فِي الدُّنْيَا وَلَا فِي الْاٰخِرَةِ وَاَنَّ مَرَدَّنَآ اِلَى اللّٰهِ وَاَنَّ الْمُسْرِفِيْنَ هُمْ اَصْحٰبُ النَّارِ ﴿٤٣﴾

45. Basi karibuni mtayakumbuka ninayowaambieni; nami ninamkabidhi Allah jambo langu; hakika Allah ndiye Awaonaye watu.

فَسَتَذْكُرُوْنَ مَآ اَقُوْلُ لَكُمْ ۭ وَاُفَوِّضُ اَمْرِيْٓ اِلَى اللّٰهِ ۭ اِنَّ اللّٰهَ بَصِيْرٌۢ بِالْعِبَادِ ﴿٤٤﴾

46. Na Allah Akamlinda katika ubaya wa hila walizofanya, na adhabu mbaya ikawazunguka watu wa Firauni.

فَوَقٰىهُ اللّٰهُ سَيِّاٰتِ مَا مَكَرُوْا وَحَاقَ بِاٰلِ فِرْعَوْنَ سُوْٓءُ الْعَذَابِ ﴿٤٥﴾

47. Ni Moto! wanawekwa mbele yake asubuhi na jioni. Na siku ile itakapotokea saa (itahukumiwa): Waingizeni watu wa Firauni katika adhabu kali zaidi.

اَلنَّارُ يُعْرَضُوْنَ عَلَيْهَا غُدُوًّا وَّعَشِيًّا ۚ وَيَوْمَ تَقُوْمُ السَّاعَةُ ۫ اَدْخِلُوْٓا اٰلَ فِرْعَوْنَ اَشَدَّ الْعَذَابِ ﴿٤٦﴾

48. Na watakapobishana katika moto huo ndipo wadhaifu watawaambia wale waliojitukuza: Kwa yakini sisi tulikuwa wafuasi wenu, basi je, mnawe-za kutuondolea (hata) sehemu ya Moto?

وَاِذْ يَتَحَآجُّوْنَ فِي النَّارِ فَيَقُوْلُ الضُّعَفٰٓؤُا لِلَّذِيْنَ اسْتَكْبَرُوْٓا اِنَّا كُنَّا لَكُمْ تَبَعًا فَهَلْ اَنْتُمْ مُّغْنُوْنَ عَنَّا نَصِيْبًا مِّنَ النَّارِ ﴿٤٧﴾

49. Watasema waliojitukuza: Sisi sote tumo humu, hakika Allah Amekwisha hukumu baina ya watu.

قَالَ الَّذِيْنَ اسْتَكْبَرُوْٓا اِنَّا كُلٌّ فِيْهَآ ۙ اِنَّ اللّٰهَ قَدْ حَكَمَ بَيْنَ الْعِبَادِ ﴿٤٩﴾

50. Na wale waliomo Motoni watawaambia walinzi wa Jahanamu: Mwombeni Mola wenu Atupunguzie siku moja ya adhabu.

وَقَالَ الَّذِيْنَ فِي النَّارِ لِخَزَنَةِ جَهَنَّمَ ادْعُوْا رَبَّكُمْ يُخَفِّفْ عَنَّا يَوْمًا مِّنَ الْعَذَابِ ﴿٥٠﴾

51. Watasema: Je, hawakuwa wanawafikieni Mitume wenu kwa Ishara zilizo wazi? Watasema: Ndiyo! Watasema: Basi ombeni (wenyewe). Lakini maombi ya makafiri hayawi ila kupotea bure.

قَالُوْٓا اَوَلَمْ تَكُ تَاْتِيْكُمْ رُسُلُكُمْ بِالْبَيِّنٰتِ ؕ قَالُوْا بَلٰى ؕ قَالُوْا فَادْعُوْا ۚ وَمَا دُعٰٓؤُا الْكٰفِرِيْنَ اِلَّا فِيْ ضَلٰلٍ ﴿٥١﴾ ع ١٠

FUNGU 6

52. Bila shaka Sisi Tutawasaidia Mitume Wetu na wale walioamini katika maisha ya dunia na siku watakaposimama mashahidi,

اِنَّا لَنَنْصُرُ رُسُلَنَا وَالَّذِيْنَ اٰمَنُوْا فِي الْحَيٰوةِ الدُّنْيَا وَيَوْمَ يَقُوْمُ الْاَشْهَادُ ۙ﴿٥٢﴾

53. Siku ambayo hautawafaa wadhalimu udhuru wao na watapata laana na mahali pao patakuwa pabaya.

يَوْمَ لَا يَنْفَعُ الظّٰلِمِيْنَ مَعْذِرَتُهُمْ وَلَهُمُ اللَّعْنَةُ وَلَهُمْ سُوْٓءُ الدَّارِ ﴿٥٣﴾

54. Na kwa hakika Tulimpa Musa mwongozo na Tukawarithisha wana wa Israeli Kitabu.

وَلَقَدْ اٰتَيْنَا مُوْسَى الْهُدٰى وَاَوْرَثْنَا بَنِيْٓ اِسْرَآءِيْلَ الْكِتٰبَ ۙ﴿٥٤﴾

55. (Kilichokuwa) mwongozo na ukumbusho kwa wenye akili.

هُدًى وَّذِكْرٰى لِاُولِي الْاَلْبَابِ ﴿٥٥﴾

56. Basi subiri, bila shaka ahadi ya Allah ni kweli, na uombe

فَاصْبِرْ اِنَّ وَعْدَ اللّٰهِ حَقٌّ وَّاسْتَغْفِرْ

Aya 52. Hapa Allah ameweka ahadi ya nguvu kabisa kuwa Manabii na waaminio lazima awasaidie hapa duniani mpaka Akhera hata itakuwa lazima wao washinde na mambo yao yafanikiwe.

Aya 56. *Wastaghfir lidhanbika*, "Na uombe msamaha kwa dhambi zako." Neno la Kiarabu *dhanb* ni tofauti na neno *ithm* (dhambi). Neno *dhanb* linakusanya kila namna ya upungufu unaotokea katika kutoangalia, kutokuwa na uwezo na kughafilika. Neno *ghafr* maana yake ni kukifunika kitu kwa chombo kitakachokizuia kisipate uchafu. Hivyo kwa mujibu wa neno *dhanb* maana ya maneno hayo katika Aya itakuwa hivi, "Uombe kulindwa na kila namna ya upungufu." Sio mradi wa maneno haya, kama tulivyokwisha eleza mara nyingi, kuwa Mtume s.a.w (Mungu apishe mbali) alikuwa na dhambi, hasha. (Pia tazama sura 48:3).

لِذَنْۢبِكَ وَسَبِّحْ بِحَمْدِ رَبِّكَ بِالْعَشِيِّ وَالْاِبْكَارِ ﴿٥٥﴾

msamaha kwa dhambi zako, na umtukuze Mola wako kwa kumsifu jioni na asubuhi.

اِنَّ الَّذِيْنَ يُجَادِلُوْنَ فِيْٓ اٰيٰتِ اللّٰهِ بِغَيْرِ سُلْطٰنٍ اَتٰىهُمْ ۙ اِنْ فِيْ صُدُوْرِهِمْ اِلَّا كِبْرٌ مَّا هُمْ بِبَالِغِيْهِ ۚ فَاسْتَعِذْ بِاللّٰهِ ۭ اِنَّهٗ هُوَ السَّمِيْعُ الْبَصِيْرُ ﴿٥٦﴾

57. Kwa yakini wale wanaobishana katika Aya za Allah pasipo dalili yo yote iliyowafikia, hamna cho chote mioyoni mwao ila majivuno tu ya (kutafuta) ukubwa ambao hawataupata. Basi ujikinge kwa Allah. Kwa hakika yeye ni Mwenye kusikia, Mwenye kuona.

لَخَلْقُ السَّمٰوٰتِ وَالْاَرْضِ اَكْبَرُ مِنْ خَلْقِ النَّاسِ وَلٰكِنَّ اَكْثَرَ النَّاسِ لَا يَعْلَمُوْنَ ﴿٥٧﴾

58. Kwa yakini uumbaji wa mbingu na ardhi ni mkubwa kuliko uumbaji wa wanadamu; lakini watu wengi hawajui.

وَمَا يَسْتَوِي الْاَعْمٰى وَالْبَصِيْرُ ۙ وَالَّذِيْنَ اٰمَنُوْا وَعَمِلُوا الصّٰلِحٰتِ وَلَا الْمُسِيْٓءُ ۭ قَلِيْلًا مَّا تَتَذَكَّرُوْنَ ﴿٥٨﴾

59. Na kipofu na mwenye macho hawawi sawa, na wale walioamini na kufanya wema hawawi sawa na afanyaye uovu; mnayoyakumbuka ni kidogo.

اِنَّ السَّاعَةَ لَاٰتِيَةٌ لَّا رَيْبَ فِيْهَا وَلٰكِنَّ اَكْثَرَ النَّاسِ لَا يُؤْمِنُوْنَ ﴿٥٩﴾

60. Kwa yakini saa lazima itafika, nayo haina shaka, lakini watu wengi hawaamini.

وَقَالَ رَبُّكُمُ ادْعُوْنِيْٓ اَسْتَجِبْ لَكُمْ ۭ اِنَّ الَّذِيْنَ يَسْتَكْبِرُوْنَ عَنْ عِبَادَتِيْ سَيَدْخُلُوْنَ جَهَنَّمَ دٰخِرِيْنَ ﴿٦٠﴾ ع ١١

61. Na Mola wenu Husema: Niombeni Nitawajibuni. Kwa hakika wale wajiivunao kufanya ibada Yangu, wao bila shaka karibuni wataingia Jahanamu wakifedheheka.

FUNGU 7

اَللّٰهُ الَّذِيْ جَعَلَ لَكُمُ الَّيْلَ لِتَسْكُنُوْا فِيْهِ وَالنَّهَارَ مُبْصِرًا ۭ اِنَّ اللّٰهَ لَذُوْ فَضْلٍ عَلَى النَّاسِ وَلٰكِنَّ اَكْثَرَ النَّاسِ لَا يَشْكُرُوْنَ ﴿٦١﴾

62. Allah Ndiye Aliyewafanyieni usiku ili mtulie humo, na mchana wenye kuangaza; hakika Allah ni Mwenye kuwafadhili sana watu, lakini watu wengi hawashukuru.

Aya 61. *Niombeni Nitawajibuni.* Kumwomba Allah ndiyo njia mojawapo ya kumzidishia mtu yakini kuwa kweli Allah yupo. Mtu atakapoomba na Mungu atakapomjibu, bila shaka imani yake itazidi na mapenzi yake kwa Allah pia yatazidi. Neno *Ud-'uuni* (niombeni) pia maana yake ni *Niabuduni* (Baidhawi).

63. Huyo Ndiye Allah, Mola wenu, Mwumba wa kila kitu, hakuna aabudiwaye ila Yeye; basi mnageuzwa wapi?

ذٰلِكُمُ اللّٰهُ رَبُّكُمْ خَالِقُ كُلِّ شَيْءٍ ۖ لَآ اِلٰهَ اِلَّا هُوَ ۚ فَاَنّٰى تُؤْفَكُوْنَ ﴿٦٢﴾

64. Kadhalika ndivyo walivyogeuzwa wale waliokuwa wakizikataa Aya za Allah.

كَذٰلِكَ يُؤْفَكُ الَّذِيْنَ كَانُوْا بِاٰيٰتِ اللّٰهِ يَجْحَدُوْنَ ﴿٦٣﴾

65. Allah ndiye Aliyewafanyieni ardhi mahali pa kustarehe, na mbingu kuwa dari, na Akazitengeneza sura zenu kisha Akazifanya vizuri sura zenu, na Akawaruzukuni katika vitu vizuri; Huyo ndiye Allah, Mola wenu; basi Mwenye baraka ni Allah, Mola wa walimwengu wote.

اَللّٰهُ الَّذِيْ جَعَلَ لَكُمُ الْاَرْضَ قَرَارًا وَّالسَّمَآءَ بِنَآءً وَّ صَوَّرَكُمْ فَاَحْسَنَ صُوَرَكُمْ وَرَزَقَكُمْ مِّنَ الطَّيِّبٰتِ ؕ ذٰلِكُمُ اللّٰهُ رَبُّكُمْ ۚ فَتَبٰرَكَ اللّٰهُ رَبُّ الْعٰلَمِيْنَ ﴿٦٤﴾

66. Yeye ndiye Hai, hakuna aabudiwaye ila Yeye, kwa hiyo Mwombeni mkimhalisishia utii; sifa zote njema ni za Allah, Mola wa viumbe vyote.

هُوَ الْحَيُّ لَآ اِلٰهَ اِلَّا هُوَ فَادْعُوْهُ مُخْلِصِيْنَ لَهُ الدِّيْنَ ؕ اَلْحَمْدُ لِلّٰهِ رَبِّ الْعٰلَمِيْنَ ﴿٦٥﴾

67. Sema: Hakika nimekatazwa kuwaabudu wale mnaowaita (kuwa miungu) badala ya Allah ziliponifikia Ishara zilizo bayana kutoka kwa Mola wangu; na nimeamrishwa nijitupe kwa Mola wa walimwengu.

قُلْ اِنِّيْ نُهِيْتُ اَنْ اَعْبُدَ الَّذِيْنَ تَدْعُوْنَ مِنْ دُوْنِ اللّٰهِ لَمَّا جَآءَنِيَ الْبَيِّنٰتُ مِنْ رَّبِّيْ ۖ وَاُمِرْتُ اَنْ اُسْلِمَ لِرَبِّ الْعٰلَمِيْنَ ﴿٦٦﴾

68. Yeye ndiye Aliyewaumbeni kwa udongo, kisha kwa manii, kisha kwa pande la damu, halafu Akawatoeni katika hali ya mtoto mchanga, kisha (Akawaacheni) ili mpate nguvu zenu kamili, kisha muwe wazee; na wengine wenu hufishwa kabla (ya uzee), na ili mfikie muda uliowekwa, na ili mpate kufahamu.

هُوَ الَّذِيْ خَلَقَكُمْ مِّنْ تُرَابٍ ثُمَّ مِنْ نُّطْفَةٍ ثُمَّ مِنْ عَلَقَةٍ ثُمَّ يُخْرِجُكُمْ طِفْلًا ثُمَّ لِتَبْلُغُوْٓا اَشُدَّكُمْ ثُمَّ لِتَكُوْنُوْا شُيُوْخًا ۚ وَمِنْكُمْ مَّنْ يُّتَوَفّٰى مِنْ قَبْلُ وَلِتَبْلُغُوْٓا اَجَلًا مُّسَمًّى وَّ لَعَلَّكُمْ تَعْقِلُوْنَ ﴿٦٧﴾

69. Yeye ndiye Anayehuisha na kufisha, na anapokidhia jambo lo lote, basi Hulisemea: Kuwa, nalo huwa.

هُوَ الَّذِيْ يُحْيٖ وَيُمِيْتُ ۚ فَاِذَا قَضٰٓى اَمْرًا فَاِنَّمَا يَقُوْلُ لَهٗ كُنْ فَيَكُوْنُ ﴿٦٨﴾ ع ١٣

FUNGU 8

70. Je, huwaoni wale wanaobishana katika Aya za Allah: wanageuziwa wapi?

اَلَمْ تَرَ اِلَى الَّذِيْنَ يُجَادِلُوْنَ فِيْٓ اٰيٰتِ اللّٰهِ ؕ اَنّٰى يُصْرَفُوْنَ ۙ﴿۶۹﴾

71. Ambao wamekadhibisha Kitabu na yale Tuliyowatuma nayo Mitume Wetu; lakini karibuni watajua,

الَّذِيْنَ كَذَّبُوْا بِالْكِتٰبِ وَبِمَآ اَرْسَلْنَا بِهٖ رُسُلَنَا ۚ فَسَوْفَ يَعْلَمُوْنَ ۙ﴿۷۰﴾

72. Zitakapokuwa pingu mashingoni mwao na minyororo; watabururwa.

اِذِ الْاَغْلٰلُ فِيْٓ اَعْنَاقِهِمْ وَالسَّلٰسِلُ ؕ يُسْحَبُوْنَ ۙ﴿۷۱﴾

73. Ndani ya maji yachemkayo, kisha watatupwa Motoni.

فِى الْحَمِيْمِ ۙ ثُمَّ فِى النَّارِ يُسْجَرُوْنَ ۚ﴿۷۲﴾

74. Tena wataambiwa: Wako wapi mliokuwa mkiwashirikisha,

ثُمَّ قِيْلَ لَهُمْ اَيْنَ مَا كُنْتُمْ تُشْرِكُوْنَ ۙ﴿۷۳﴾

75. Badala ya Allah? Watasema: Wametupotea, bali toka zamani hatukuwa tunaabudu cho chote. Hivyo ndivyo Allah Huwapoteza makafiri.

مِنْ دُوْنِ اللّٰهِ ؕ قَالُوْا ضَلُّوْا عَنَّا بَلْ لَّمْ نَكُنْ نَّدْعُوْا مِنْ قَبْلُ شَيْـًٔا ؕ كَذٰلِكَ يُضِلُّ اللّٰهُ الْكٰفِرِيْنَ ۙ﴿۷۴﴾

76. Hayo ni kwa sababu mlikuwa mkifurahi katika ardhi pasipo haki, na kwa sababu mlikuwa mkijivuna.

ذٰلِكُمْ بِمَا كُنْتُمْ تَفْرَحُوْنَ فِى الْاَرْضِ بِغَيْرِ الْحَقِّ وَبِمَا كُنْتُمْ تَمْرَحُوْنَ ۚ﴿۷۵﴾

77. Iingieni milango ya Jahanamu mkakae humo; basi ni baya lilioje kao la wanaotakabari!

اُدْخُلُوْٓا اَبْوَابَ جَهَنَّمَ خٰلِدِيْنَ فِيْهَا ۚ فَبِئْسَ مَثْوَى الْمُتَكَبِّرِيْنَ ﴿۷۶﴾

78. Basi subiri, hakika ahadi ya Allah ni kweli; na kama Tukikuonyesha baadhi ya yale Tuliyowaahidi au Tukikufisha, basi watarudishwa Kwetu.

فَاصْبِرْ اِنَّ وَعْدَ اللّٰهِ حَقٌّ ۚ فَاِمَّا نُرِيَنَّكَ بَعْضَ الَّذِىْ نَعِدُهُمْ اَوْ نَتَوَفَّيَنَّكَ فَاِلَيْنَا يُرْجَعُوْنَ ﴿۷۷﴾

79. Na kwa yakini Tuliwatuma Mitume kabla yako, wengine wao Tumekusimulia na wengine wao Hatukukusimulia; na haikuwa kwa Mtume ye yote kuleta Ishara ila kwa idhini ya Allah. Na itakapofika hukumu ya Allah itahukumiwa kwa haki, na washikao batili hapo watapata hasara.

وَلَقَدْ اَرْسَلْنَا رُسُلًا مِّنْ قَبْلِكَ مِنْهُمْ مَّنْ قَصَصْنَا عَلَيْكَ وَمِنْهُمْ مَّنْ لَّمْ نَقْصُصْ عَلَيْكَ ؕ وَمَا كَانَ لِرَسُوْلٍ اَنْ يَّاْتِىَ بِاٰيَةٍ اِلَّا بِاِذْنِ اللّٰهِ ۚ فَاِذَا جَآءَ اَمْرُ اللّٰهِ قُضِىَ بِالْحَقِّ وَخَسِرَ هُنَالِكَ الْمُبْطِلُوْنَ ﴿۷۸﴾ ع ۱۳

Aya 79. *Na wengine Hatukukusimulia.* Kwa hakika Kurani si Kitabu cha tarehe au historia

FUNGU 9

اَللّٰهُ الَّذِیْ جَعَلَ لَكُمُ الْاَنْعَامَ لِتَرْكَبُوْا مِنْهَا وَمِنْهَا تَاْكُلُوْنَ ﴿٨٠﴾

80. Allah ndiye Aliyewafanyieni wanyama ili mwapande baadhi yao na wengine wao mpate kuwala.

وَلَكُمْ فِیْهَا مَنَافِعُ وَلِتَبْلُغُوْا عَلَیْهَا حَاجَةً فِیْ صُدُوْرِكُمْ وَعَلَیْهَا وَعَلَى الْفُلْكِ تُحْمَلُوْنَ ﴿٨١﴾

81. Na katika hao mnayo manufaa; na mkapate kwao haja iliyomo vifuani mwenu, na mnachukuliwa juu yao na juu ya merikebu.

وَیُرِیْكُمْ اٰیٰتِهٖ ۫ فَاَیَّ اٰیٰتِ اللّٰهِ تُنْكِرُوْنَ ﴿٨٢﴾

82. Naye Huwaonyesheni Ishara Zake: basi mtakataa ipi katika Ishara za Allah?

اَفَلَمْ یَسِیْرُوْا فِی الْاَرْضِ فَیَنْظُرُوْا كَیْفَ كَانَ عَاقِبَةُ الَّذِیْنَ مِنْ قَبْلِهِمْ ؕ كَانُوْۤا اَكْثَرَ مِنْهُمْ وَاَشَدَّ قُوَّةً وَّاٰثَارًا فِی الْاَرْضِ فَمَاۤ اَغْنٰى عَنْهُمْ مَّا كَانُوْا یَكْسِبُوْنَ ﴿٨٣﴾

83. Je, hawajasafiri katika ardhi ili waone umekuwaje mwisho wa wale waliokuwa kabla yao? Wao walikuwa wengi kuliko hao na wenye nguvu zaidi na katika kuacha athari za (taadhima) ardhini; lakini hayakuwafaa yale waliyoyachuma.

فَلَمَّا جَآءَتْهُمْ رُسُلُهُمْ بِالْبَیِّنٰتِ فَرِحُوْا بِمَا عِنْدَهُمْ مِّنَ الْعِلْمِ وَحَاقَ بِهِمْ مَّا كَانُوْا بِهٖ یَسْتَهْزِءُوْنَ ﴿٨٤﴾

84. Basi walipowafikia Mitume wao kwa dalili zilizo wazi wakafurahia elimu waliyokuwa nayo, na yakawazunguka waliyoyafanyia mzaha.

فَلَمَّا رَاَوْا بَاْسَنَا قَالُوْۤا اٰمَنَّا بِاللّٰهِ وَحْدَهٗ وَكَفَرْنَا بِمَا كُنَّا بِهٖ مُشْرِكِیْنَ ﴿٨٥﴾

85. Lakini walipoiona adhabu Yetu wakasema: Tunamwamini Allah pekee na tunawakataa (miungu) tuliokuwa tukiwashirikisha naye.

فَلَمْ یَكُ یَنْفَعُهُمْ اِیْمَانُهُمْ لَمَّا رَاَوْا بَاْسَنَا ؕ سُنَّتَ اللّٰهِ الَّتِیْ قَدْ خَلَتْ فِیْ عِبَادِهٖ ۚ وَخَسِرَ هُنَالِكَ الْكٰفِرُوْنَ ﴿٨٥﴾ ع ١٤ ٧

86. Lakini imani yao haikuwa yenye kuwafaa walipoiona adhabu Yetu; hii ni kawaida ya Allah iliyopita katika watu Wake, na hapo waliokufuru wakapata hasara.

---

ya kuwa kilazimike kutaja habari za Manabii wote waliopita duniani. Kimechagua baadhi ya Manabii wasiopungua ishirini na tano kwa ajili ya kueleza mifano na kutoa mafundisho mbalimbali. Manabii waliofika duniani kama wajuavyo Waislamu ni zaidi kuliko laki moja.

Aya 83. Mara nyingi Allah anawahimiza watu waende wakaitazame dunia na wasafiri kila upande, na ya kwamba huko safarini watakutana na habari za watu wadhalimu waliowakanusha Manabii na kuwafanyia uadui kuwa wao waliangamizwa, na watu wema wakafanikiwa.

سُوْرَةُ حٰمٓ السَّجْدَةِ مَكِّيَّةٌ وَّ هِيَ مَعَ الْبَسْمَلَةِ خَمْسٌ وَّخَمْسُوْنَ اٰيَةً وَّ سِتَّةُ رُكُوْعَاتٍ

41. SURA HAA MIIM

Imeteremshwa Makka

Ina mafungu 6 na Aya 55 pamoja na Bismillahi

بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ ①

1. Kwa jina la Allah, Mwingi wa rehema, Mwingi wa ukarimu.

حٰمٓ ②

2. Asifiwaye, Atukuzwaye.

تَنْزِيْلٌ مِّنَ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ ③

3. Uteremsho utokao kwa Mwingi wa rehama, Mwingi wa ukarimu.

كِتٰبٌ فُصِّلَتْ اٰيٰتُهٗ قُرْاٰنًا عَرَبِيًّا لِّقَوْمٍ يَّعْلَمُوْنَ ④

4. Ni Kitabu ambacho aya zake zimeelezwa kinaganaga - chenye kusomwa mara kwa mara kilichobainishwa waziwazi - kwa ajili ya watu wanaojua.

بَشِيْرًا وَّنَذِيْرًا ۚ فَاَعْرَضَ اَكْثَرُهُمْ فَهُمْ لَا يَسْمَعُوْنَ ⑤

5. Kitoacho habari njema na kionyacho, lakini wengi wao wamekengeuka, kwa hiyo hawasikii.

وَقَالُوْا قُلُوْبُنَا فِيْٓ اَكِنَّةٍ مِّمَّا تَدْعُوْنَآ اِلَيْهِ وَفِيْٓ اٰذَانِنَا وَقْرٌ وَّمِنْۢ بَيْنِنَا وَبَيْنِكَ حِجَابٌ فَاعْمَلْ اِنَّنَا عٰمِلُوْنَ ⑥

6. Na wakasema: Mioyo yetu i katika vifuniko kwa yale unayotuitia, na katika masikio yetu mna uzito, na baina yetu sisi na wewe pana pazia; basi endelea na kazi yako, nasi pia tunafanya kazi.

قُلْ اِنَّمَآ اَنَا بَشَرٌ مِّثْلُكُمْ يُوْحٰٓى اِلَيَّ اَنَّمَآ اِلٰهُكُمْ اِلٰهٌ وَّاحِدٌ فَاسْتَقِيْمُوْٓا اِلَيْهِ وَاسْتَغْفِرُوْهُ ؕ وَوَيْلٌ لِّلْمُشْرِكِيْنَ ⑦

7. Sema: Bila shaka mimi ni mtu kama ninyi inafunuliwa kwangu ya kwamba Mungu wenu ni Mungu Mmoja tu, basi simameni imara mbele Yake na mkamtake samahani, na ole kwa washirikina.

الَّذِيْنَ لَا يُؤْتُوْنَ الزَّكٰوةَ وَهُمْ بِالْاٰخِرَةِ هُمْ كٰفِرُوْنَ ⑧

8. Ambao hawatoi Zaka nao ndio wenye kuikataa Akhera.

Sura hii inaitwa *Haa Miim* au *Haa Miim Fussilat* au *Fussilat* tu. Ilishuka Makka.

Aya 2. *Haa Miim,* "Asifiwaye, Atukuzwaye." Hizi ni herufi za mkato kwa ajili ya sifa za Allah. Haa ni *Hafiidh* au *Hamiid* (Mhifadhi au Msifiwa) na *Miim* ni *Majiid* (Atukuzwaye).

Aya 7-8. Wasiotoa Zaka hapa wameitwa ni washirikina wamshirikishao Allah, na ya kuwa hawaamini Akhera nao wanaonywa kuwa wataadhibiwa.

9. Kwa yakini wale wanaoamini na kutenda mema utakuwa kwao ujira usiokoma.

اِنَّ الَّذِيْنَ اٰمَنُوْا وَعَمِلُوا الصّٰلِحٰتِ لَهُمْ اَجْرٌ غَيْرُ مَمْنُوْنٍ ﴿٩﴾ ع ١٥

FUNGU 2

10. Sema: Je, kwa yakini mnamkataa Aliyeiumba ardhi katika nyakati mbili, na mnamfanyia washirika? Huyo ndiye Mola wa walimwengu.

قُلْ اَئِنَّكُمْ لَتَكْفُرُوْنَ بِالَّذِىْ خَلَقَ الْاَرْضَ فِىْ يَوْمَيْنِ وَتَجْعَلُوْنَ لَهٗۤ اَنْدَادًا ؕ ذٰلِكَ رَبُّ الْعٰلَمِيْنَ ﴿١٠﴾ ع

11. Akaweka humo milima juu ya uso wake kwenye sehemu zilizoinuka, na Akaweka humo baraka, na Akakadiria humo chakula chake katika nyakati nne bila tofauti kwa watafutaji wote.

وَجَعَلَ فِيْهَا رَوَاسِىَ مِنْ فَوْقِهَا وَبٰرَكَ فِيْهَا وَقَدَّرَ فِيْهَاۤ اَقْوَاتَهَا فِىْۤ اَرْبَعَةِ اَيَّامٍ ؕ سَوَآءً لِّلسَّآئِلِيْنَ ﴿١١﴾

12. Kisha akaielekea mbingu na hali i moshi, basi Akaiambia (mbingu) na ardhi: Njooni mkipenda au msipende; vyote viwili vikasema: Tunakuja kwa kupenda.

ثُمَّ اسْتَوٰۤى اِلَى السَّمَآءِ وَهِىَ دُخَانٌ فَقَالَ لَهَا وَلِلْاَرْضِ ائْتِيَا طَوْعًا اَوْ كَرْهًا ؕ قَالَتَاۤ اَتَيْنَا طَآئِعِيْنَ ﴿١٢﴾

13. Basi Akazitengeneza mbingu saba katika nyakati mbili, na kila mbingu Akaifunulia kazi yake: na Tumeipamba mbingu ya karibu kwa mataa na kuilinda; hiki ndicho kipimo cha Mwenye ushindi kamili, Mwenye kujua.

فَقَضٰٮهُنَّ سَبْعَ سَمٰوَاتٍ فِىْ يَوْمَيْنِ وَاَوْحٰى فِىْ كُلِّ سَمَآءٍ اَمْرَهَا ؕ وَزَيَّنَّا السَّمَآءَ الدُّنْيَا بِمَصَابِيْحَ ۖ وَحِفْظًا ؕ ذٰلِكَ تَقْدِيْرُ الْعَزِيْزِ الْعَلِيْمِ ﴿١٣﴾

14. Basi kama wakigeuka useme: Nawahadharisheni na adhabu mfano wa adhabu ya Waadi na Wathamudi.

فَاِنْ اَعْرَضُوْا فَقُلْ اَنْذَرْتُكُمْ صٰعِقَةً مِّثْلَ صٰعِقَةِ عَادٍ وَّثَمُوْدَ ﴿١٤﴾

15. Walipowafikia Mitume mbele yao na nyuma yao, (wakawaambia): Msiabudu ila Allah. Wakasema Angalitaka Mola wetu bila shaka Angeteremsha Malaika, na hakika sisi tunayakataa mliyotumwa nayo.

اِذْ جَآءَتْهُمُ الرُّسُلُ مِنْۢ بَيْنِ اَيْدِيْهِمْ وَمِنْ خَلْفِهِمْۤ اَلَّا تَعْبُدُوْۤا اِلَّا اللّٰهَ ؕ قَالُوْا لَوْ شَآءَ رَبُّنَا لَاَنْزَلَ مَلٰٓئِكَةً فَاِنَّا بِمَاۤ اُرْسِلْتُمْ بِهٖ كٰفِرُوْنَ ﴿١٥﴾

Zaka ni sehemu ndogo ya mali anayotakiwa kutoa mtu kila mwaka toka katika mali yake inapokuwa imefikia kiwango maalum kilichopitiwa na mwaka mmoja.

فَاَمَّا عَادٌ فَاسْتَكْبَرُوْا فِي الْاَرْضِ بِغَيْرِ الْحَقِّ وَقَالُوْا مَنْ اَشَدُّ مِنَّا قُوَّةً ؕ اَوَلَمْ يَرَوْا اَنَّ اللّٰهَ الَّذِيْ خَلَقَهُمْ هُوَ اَشَدُّ مِنْهُمْ قُوَّةً ؕ وَكَانُوْا بِاٰيٰتِنَا يَجْحَدُوْنَ ﴿۱۵﴾

16. Na ama Waadi walitakabari katika ardhi bila haki na wakasema: Ni nani aliye na nguvu zaidi kuliko sisi? Je, hawakuona ya kwamba Allah Aliyewaumba ni Mwenye nguvu zaidi kuliko wao? Nao walikuwa wakizikataa Ishara Zetu.

فَاَرْسَلْنَا عَلَيْهِمْ رِيْحًا صَرْصَرًا فِيْۤ اَيَّامٍ نَّحِسَاتٍ لِّنُذِيْقَهُمْ عَذَابَ الْخِزْيِ فِي الْحَيٰوةِ الدُّنْيَا ؕ وَلَعَذَابُ الْاٰخِرَةِ اَخْزٰى وَهُمْ لَا يُنْصَرُوْنَ ﴿۱۶﴾

17. Basi Tuliwatumia upepo mkali katika siku za mkosi ili Tuwaonjeshe adhabu ya fedheha katika maisha ya dunia; na bila shaka adhabu ya Akhera yafedhehesha zaidi, nao hawatasaidiwa.

وَاَمَّا ثَمُوْدُ فَهَدَيْنٰهُمْ فَاسْتَحَبُّوا الْعَمٰى عَلَى الْهُدٰى فَاَخَذَتْهُمْ صٰعِقَةُ الْعَذَابِ الْهُوْنِ بِمَا كَانُوْا يَكْسِبُوْنَ ﴿۱۷﴾

18. Na ama Wathamudi Tuliwaongoza lakini walipenda upofu kuliko kuongoka, basi mngurumo wa adhabu ifedheheshayo ukawashika kwa sababu ya yale waliyokuwa wakiyachuma.

وَنَجَّيْنَا الَّذِيْنَ اٰمَنُوْا وَكَانُوْا يَتَّقُوْنَ ﴿۱۸﴾ ع ۱۶

19. Na Tukawaokoa wale walioamini na waliokuwa wakijilinda.

FUNGU 3

وَيَوْمَ يُحْشَرُ اَعْدَآءُ اللّٰهِ اِلَى النَّارِ فَهُمْ يُوْزَعُوْنَ ﴿۱۹﴾

20. Na siku watakapokusanywa maadui wa Allah kwenye moto, nao watapangwa makundi makundi.

حَتّٰۤى اِذَا مَا جَآءُوْهَا شَهِدَ عَلَيْهِمْ سَمْعُهُمْ وَاَبْصَارُهُمْ وَجُلُوْدُهُمْ بِمَا كَانُوْا يَعْمَلُوْنَ ﴿۲۰﴾

21. Hata watakapoufikia, ndipo masikio yao, na macho yao, na ngozi zao vitatoa ushahidi dhidi yao kwa yale waliyokuwa wakiyatenda.

وَقَالُوْا لِجُلُوْدِهِمْ لِمَ شَهِدْتُّمْ عَلَيْنَا ؕ قَالُوْۤا اَنْطَقَنَا اللّٰهُ الَّذِيْۤ اَنْطَقَ كُلَّ شَيْءٍ وَّ هُوَ خَلَقَكُمْ اَوَّلَ مَرَّةٍ وَّ اِلَيْهِ تُرْجَعُوْنَ ﴿۲۱﴾

22. Nao wataziambia ngozi zao: Kwa nini mmetoa ushahidi dhidi yetu? Zitasema: Allah Aliyekitamkisha kila kitu ndiye Ametutamkisha, naye Aliwaumbeni mara ya kwanza na Kwake mtarudishwa.

وَمَا كُنْتُمْ تَسْتَتِرُوْنَ اَنْ يَّشْهَدَ عَلَيْكُمْ سَمْعُكُمْ وَلَآ اَبْصَارُكُمْ وَلَا جُلُوْدُكُمْ وَلٰكِنْ ظَنَنْتُمْ اَنَّ اللّٰهَ لَا يَعْلَمُ كَثِيْرًا مِّمَّا تَعْمَلُوْنَ ﴿٢٢﴾

23. Na hamkuwa wenye kujificha ili masikio yenu na macho yenu na ngozi zenu visitoe ushahidi dhidi yenu; bali mlidhani ya kwamba Allah Hayajui mengi katika (hayo) mnayoyafanya.

وَذٰلِكُمْ ظَنُّكُمُ الَّذِيْ ظَنَنْتُمْ بِرَبِّكُمْ اَرْدٰىكُمْ فَاَصْبَحْتُمْ مِّنَ الْخٰسِرِيْنَ ﴿٢٣﴾

24. Na hii dhana yenu mliyomdhania Mola wenu imewaangamizeni; na mmekuwa miongoni mwa wenye hasara.

فَاِنْ يَّصْبِرُوْا فَالنَّارُ مَثْوًى لَّهُمْ ۚ وَاِنْ يَّسْتَعْتِبُوْا فَمَا هُمْ مِّنَ الْمُعْتَبِيْنَ ﴿٢٤﴾

25. Hata wakisubiri basi Moto ndio kao lao; na kama wakitoa udhuru hawata-kuwa miongoni mwa wenye kukubaliwa.

وَقَيَّضْنَا لَهُمْ قُرَنَآءَ فَزَيَّنُوْا لَهُمْ مَّا بَيْنَ اَيْدِيْهِمْ وَمَا خَلْفَهُمْ وَحَقَّ عَلَيْهِمُ الْقَوْلُ فِيْٓ اُمَمٍ قَدْ خَلَتْ مِنْ قَبْلِهِمْ مِّنَ الْجِنِّ وَالْاِنْسِ ۚ اِنَّهُمْ كَانُوْا خٰسِرِيْنَ ﴿٢٥﴾ ع ١٧

26. Na Tukawawekea marafiki waliowapambia yale yaliyo mbele yao na nyuma yao; na kauli ile ile imelazimika juu yao iliyolazimika kwa mataifa yaliyokwisha pita kabla yao miongoni mwa majinni na watu; hakika wao walikuwa ni wenye hasara.

FUNGU 4

وَقَالَ الَّذِيْنَ كَفَرُوْا لَا تَسْمَعُوْا لِهٰذَا الْقُرْاٰنِ وَالْغَوْا فِيْهِ لَعَلَّكُمْ تَغْلِبُوْنَ ﴿٢٦﴾

27. Na walisema waliokufuru: Msisikilize Kurani hii na ipigieni makelele (isomwapo) huenda mtashinda.

فَلَنُذِيْقَنَّ الَّذِيْنَ كَفَرُوْا عَذَابًا شَدِيْدًا ۙ وَّلَنَجْزِيَنَّهُمْ اَسْوَاَ الَّذِيْ كَانُوْا يَعْمَلُوْنَ ﴿٢٧﴾

28. Basi kwa hakika Tutawaonjesha wale waliokufuru adhabu kali na kwa yakini Tutawalipa malipo mabaya ya yale waliyokuwa wakiyafanya.

ذٰلِكَ جَزَآءُ اَعْدَآءِ اللّٰهِ النَّارُ ۚ لَهُمْ فِيْهَا دَارُ الْخُلْدِ ۭ جَزَآءًۢ بِمَا كَانُوْا بِاٰيٰتِنَا يَجْحَدُوْنَ ﴿٢٨﴾

29. Hayo ndiyo malipo ya maadui wa Allah - Moto; humo watakuwa na nyumba ya kukaa muda mrefu; ndiyo malipo kwa sababu walikuwa wakizikataa Aya Zetu.

Aya 27. Makafiri wa Makka walikuwa wakipiga kelele iliposomwa Kurani. Hii ndiyo hila nyingine ya makafiri ya kwamba wasisikilize maneno ya ubashiri wanayoambiwa au kusomewa, na kuvuruga mazungumzo kwa kupiga kelele ili watu wasiisikilize haki ikawavuta; wanafikiri wakifanya hivi wakweli watachoka kueleza haki nao watashinda.

30. Na wale waliokufuru watasema: Mola wetu, Utuonyeshe (makundi) mawili yaliyotupoteza miongoni mwa majinni na watu ili tuwapondeponde chini ya miguu yetu, wapate kuwa miongoni mwa waliodhalilika kabisa.

وَقَالَ الَّذِيْنَ كَفَرُوْا رَبَّنَآ اَرِنَا الَّذَيْنِ اَضَلّٰنَا مِنَ الْجِنِّ وَالْاِنْسِ نَجْعَلْهُمَا تَحْتَ اَقْدَامِنَا لِيَكُوْنَا مِنَ الْاَسْفَلِيْنَ ﴿٢٩﴾

31. Hakika wale wanaosema, Mola wetu ni Allah, kisha wakaendelea kwa kudumu, huwateremkia Malaika (wakiwaambia): Msiogope wala msihuzunike, na ifurahieni Pepo mliyokuwa mkiahidiwa.

اِنَّ الَّذِيْنَ قَالُوْا رَبُّنَا اللّٰهُ ثُمَّ اسْتَقَامُوْا تَتَنَزَّلُ عَلَيْهِمُ الْمَلٰٓئِكَةُ اَلَّا تَخَافُوْا وَلَا تَحْزَنُوْا وَاَبْشِرُوْا بِالْجَنَّةِ الَّتِيْ كُنْتُمْ تُوْعَدُوْنَ ﴿٣٠﴾

32. Sisi ni marafiki wenu katika maisha ya dunia na katika Akhera, na humo mtapata vitu zinavyovipenda nafsi zenu na humo mtapata mtakavyoviomba.

نَحْنُ اَوْلِيٰٓؤُكُمْ فِي الْحَيٰوةِ الدُّنْيَا وَفِي الْاٰخِرَةِ ۚ وَلَكُمْ فِيْهَا مَا تَشْتَهِيْٓ اَنْفُسُكُمْ وَلَكُمْ فِيْهَا مَا تَدَّعُوْنَ ﴿٣١﴾

33. Ni karibisho litokalo kwa Msamehevu, Mwenye rehema.

نُزُلًا مِّنْ غَفُوْرٍ رَّحِيْمٍ ﴿٣٢﴾ ع ١٨

FUNGU 5

34. Na ni nani atoaye kauli bora zaidi kuliko aitaye kwa Allah na kufanya vitendo vizuri na husema: Hakika mimi ni miongoni mwa watii.

وَمَنْ اَحْسَنُ قَوْلًا مِّمَّنْ دَعَآ اِلَى اللّٰهِ وَعَمِلَ صَالِحًا وَّقَالَ اِنَّنِيْ مِنَ الْمُسْلِمِيْنَ ﴿٣٣﴾

35. Hauwezi kuwa sawa wema na uovu. Zuia (ubaya) kwa yaliyo mema zaidi, hapo yule ambaye baina yako na yeye pana uadui atakuwa kama ni rafiki sana.

وَلَا تَسْتَوِي الْحَسَنَةُ وَلَا السَّيِّئَةُ ۭ اِدْفَعْ بِالَّتِيْ هِيَ اَحْسَنُ فَاِذَا الَّذِيْ بَيْنَكَ وَبَيْنَهٗ عَدَاوَةٌ كَاَنَّهٗ وَلِيٌّ حَمِيْمٌ ﴿٣٤﴾

Aya 31. Aya hii inaonyesha ya kuwa waliomwamini Allah na wakashikilia imani yao imara, katika taabu na dhiki, wao hushukiwa na Malaika hapa hapa duniani ambao wanawaambia maneno ya kuwafariji. Aya 32 inahakikisha jambo hili.

Aya 34. Watu wanaofanya kazi ya kuwaita watu kwenye dini ya Allah na kwenye ibada na kazi Yake, wanasemwa wao ndio wenye kauli bora. Laiti Waislamu wangeshika kazi hii ya kuwaita watu kwenye haki na kusimamisha vitendo vizuri.

وَمَا يُلَقّٰىهَآ اِلَّا الَّذِيْنَ صَبَرُوْا ۚ وَمَا يُلَقّٰىهَآ اِلَّا ذُوْ حَظٍّ عَظِيْمٍ ﴿٣٥﴾

36. Lakini (jambo hili) halitapewa ila wale wenye subira, wala halitapewa ila mwenye bahati kubwa.

وَاِمَّا يَنْزَغَنَّكَ مِنَ الشَّيْطٰنِ نَزْغٌ فَاسْتَعِذْ بِاللّٰهِ ؕ اِنَّهٗ هُوَ السَّمِيْعُ الْعَلِيْمُ ﴿٣٦﴾

37. Na kama shetani akikushawishi kwa tashwishi, basi jikinge kwa Allah; bila shaka Yeye ni Mwenye kusikia, Mwenye kujua.

وَمِنْ اٰيٰتِهِ الَّيْلُ وَالنَّهَارُ وَالشَّمْسُ وَالْقَمَرُ ؕ لَا تَسْجُدُوْا لِلشَّمْسِ وَلَا لِلْقَمَرِ وَاسْجُدُوْا لِلّٰهِ الَّذِيْ خَلَقَهُنَّ اِنْ كُنْتُمْ اِيَّاهُ تَعْبُدُوْنَ ﴿٣٧﴾

38. Na katika Ishara Zake ni usiku na mchana na jua na mwezi; msilisujudie jua wala mwezi; bali msujudieni Allah Aliyeviumba; ikiwa ninyi mnamwabudu Yeye tu.

فَاِنِ اسْتَكْبَرُوْا فَالَّذِيْنَ عِنْدَ رَبِّكَ يُسَبِّحُوْنَ لَهٗ بِالَّيْلِ وَالنَّهَارِ وَهُمْ لَا يَسْـَٔمُوْنَ ﴿٣٨﴾ ۩

39. Na kama wakitakabari, basi walioko kwa Mola wako wanamsabihi usiku na mchana, nao hawachoki.

وَمِنْ اٰيٰتِهٖٓ اَنَّكَ تَرَى الْاَرْضَ خَاشِعَةً فَاِذَآ اَنْزَلْنَا عَلَيْهَا الْمَآءَ اهْتَزَّتْ وَرَبَتْ ؕ اِنَّ الَّذِيْٓ اَحْيَاهَا لَمُحْيِ الْمَوْتٰى ؕ اِنَّهٗ عَلٰى كُلِّ شَيْءٍ قَدِيْرٌ ﴿٣٩﴾

40. Na katika ishara Zake ni kwamba unaiona ardhi imenyauka, lakini Tunapoiteremshia maji inahuika na kuumuka. Bila shaka Yule Aliyeihuisha kwa yakini ni mwenye kuhuisha wafu. Hakika Yeye Ndiye Mwenye uwezo juu ya kila kitu.

اِنَّ الَّذِيْنَ يُلْحِدُوْنَ فِيْٓ اٰيٰتِنَا لَا يَخْفَوْنَ عَلَيْنَا ؕ اَفَمَنْ يُّلْقٰى فِي النَّارِ خَيْرٌ اَمْ مَّنْ يَّاْتِيْٓ اٰمِنًا يَّوْمَ الْقِيٰمَةِ ؕ اِعْمَلُوْا مَا شِئْتُمْ ۙ اِنَّهٗ بِمَا تَعْمَلُوْنَ بَصِيْرٌ ﴿٤٠﴾

41. Kwa yakini wale wanaokwenda upande katika Ishara Zetu hawafichiki kwetu. Je, atakayetupwa Motoni ni bora au atakayekuja kwa amani siku ya Kiyama? Fanyeni mnavyopenda, kwa yakini Yeye Anayaona mnayoyafanya.

اِنَّ الَّذِيْنَ كَفَرُوْا بِالذِّكْرِ لَمَّا جَآءَهُمْ ۚ وَاِنَّهٗ لَكِتٰبٌ عَزِيْزٌ ﴿٤١﴾ ۙ

42. Kwa hakika wale wanaoukataa ukumbusho uwafikiapo, na bila shaka huo ni Kitabu kiheshimiwacho.

لَّا يَاْتِيْهِ الْبَاطِلُ مِنْۢ بَيْنِ يَدَيْهِ وَلَا مِنْ خَلْفِهٖ ؕ تَنْزِيْلٌ مِّنْ حَكِيْمٍ حَمِيْدٍ ﴿٤٢﴾

43. Uongo hautakifikia mbele yake wala nyuma yake; kimeteremshwa na Mwenye hekima, Ahimidiwaye.

Aya 43. Dunia na iendelee namna gani katika sayansi na maarifa haitaweza kubatilisha fundisho lo lote la Kurani kuwa si sahihi. Na majira yapinduke na yageuke namna gani

مَا يُقَالُ لَكَ اِلَّا مَا قَدْ قِيْلَ لِلرُّسُلِ مِنْ قَبْلِكَ ؕ اِنَّ رَبَّكَ لَذُوْ مَغْفِرَةٍ وَّذُوْ عِقَابٍ اَلِيْمٍ ﴿٤٣﴾

44. Huambiwi ila yale yale waliyoambiwa Mitume wa kabla yako; kwa yakini Mola wako ni Mwenye kusamehe na Mwenye adhabu iumizayo.

وَلَوْ جَعَلْنٰهُ قُرْاٰنًا اَعْجَمِيًّا لَّقَالُوْا لَوْلَا فُصِّلَتْ اٰيٰتُهٗ ؕ ءَاَعْجَمِيٌّ وَّعَرَبِيٌّ ؕ قُلْ هُوَ لِلَّذِيْنَ اٰمَنُوْا هُدًى وَّشِفَآءٌ ؕ وَالَّذِيْنَ لَا يُؤْمِنُوْنَ فِيْٓ اٰذَانِهِمْ وَقْرٌ وَّهُوَ عَلَيْهِمْ عَمًى ؕ اُولٰٓئِكَ يُنَادَوْنَ مِنْ مَّكَانٍۢ بَعِيْدٍ ﴿٤٤﴾ ع ١٩

45. Na lau kama Tungaliifanya Kurani kwa lugha ya kigeni bila shaka wangalisema: Kwa nini Aya zake hazikupambanuliwa? Je! lugha ya kigeni na Mwarabu vinafanana? Sema: Hiyo ni mwongozo na ponyo kwa wale walioamini ; na wale wasioamini kuna uziwi masikioni mwao unaosababisha ifichike kwao; hao ndio watakaoitwa kutoka mahali pa mbali.

FUNGU 6

وَلَقَدْ اٰتَيْنَا مُوْسَى الْكِتٰبَ فَاخْتُلِفَ فِيْهِ ؕ وَلَوْلَا كَلِمَةٌ سَبَقَتْ مِنْ رَّبِّكَ لَقُضِيَ بَيْنَهُمْ ؕ وَاِنَّهُمْ لَفِيْ شَكٍّ مِّنْهُ مُرِيْبٍ ﴿٤٥﴾

46. Na hakika Tulimpa Musa Kitabu, lakini ikahitilafiwa kwacho; na lau isingekuwa kauli iliyotangulia kutoka kwa Mola wako, hukumu ingalikatwa baina yao; na kwa yakini wao wamo katika shaka nacho ihangaishayo.

مَنْ عَمِلَ صَالِحًا فَلِنَفْسِهٖ ۚ وَمَنْ اَسَآءَ فَعَلَيْهَا ؕ وَمَا رَبُّكَ بِظَلَّامٍ لِّلْعَبِيْدِ ﴿٤٦﴾

47. Mwenye kutenda mema ni kwa nafsi yake, na mwenye kutenda ubaya ni juu ya nafsi yake; na Mola wako si mwenye kuwadhulumu hata kidogo watumishi.

---

haitawezekana kubadilisha maneno ya Kurani kwa maneno yo yote mengineyo. Sura hii imeanza na sifa ya Allah *Hafiidh* (Mhifadhi) na hapa imeonyeshwa ya kuwa Kurani imehifadhiwa katika kila hali.

Aya 45. *Ponyo.* Kwa hakika Kurani imejihakikisha kuwa ponyo la magonjwa ya kiroho. Imewafanya watu waliokuwa katika hali ya chini kabisa ya kibinadamu waeneze ustaarabu wa dini na wa kidunia katika muda mdogo wa miaka 25.

Aya 46. *Hukumu ingalikatwa baina yao,* yaani wangeadhibiwa. *Kauli iliyotangulia* ni ya kwamba Allah hawaadhibu watu na hali Nabii yumo miongoni mwao (sura 8:34).

Aya 47. Aya hii inaonyesha ya kwamba kama mtu anafanya wema, basi wema huo utamfaa yeye mwenyewe, si kama wema wake utamfaa Allah, hasha. Na kama akitenda ubaya basi ni mwenyewe anaidhuru nafsi yake.

JUZU 25

48. Elimu ya saa ile inarudishwa Kwake. Na (baadhi ya) matunda hayatoki katika vifuniko vyake wala mwanamke hapati mimba wala hazai ila kwa elimu Yake; na siku Atakayowaita, (Akisema): Wako wapi washirika wangu? Watasema: Twakiri Kwako kwamba hakuna shahidi miongoni mwetu.

اِلَيۡهِ يُرَدُّ عِلۡمُ السَّاعَةِ ؕ وَمَا تَخۡرُجُ مِنۡ ثَمَرٰتٍ مِّنۡ اَكۡمَامِهَا وَمَا تَحۡمِلُ مِنۡ اُنۡثٰى وَلَا تَضَعُ اِلَّا بِعِلۡمِهٖ ؕ وَيَوۡمَ يُنَادِيۡهِمۡ اَيۡنَ شُرَكَآءِىۡ ؕ قَالُوۡۤا اٰذَنّٰكَ ؕ مَا مِنَّا مِنۡ شَهِيۡدٍ ۚ﴿۴۸﴾

49. Na vyote vile walivyokuwa wakiviomba hapo kabla vitawapotea, na watadhani ya kwamba hawana pa kukimbilia.

وَضَلَّ عَنۡهُمۡ مَّا كَانُوۡا يَدۡعُوۡنَ مِنۡ قَبۡلُ وَظَنُّوۡا مَا لَهُمۡ مِّنۡ مَّحِيۡصٍ ﴿۴۹﴾

50. Mwanadamu hachoki kuomba dua ya heri, na inapompata shari, basi hukata tamaa kabisa na kuwa asiye na matumaini.

لَا يَسۡـَٔمُ الۡاِنۡسَانُ مِنۡ دُعَآءِ الۡخَيۡرِ ۫ وَاِنۡ مَّسَّهُ الشَّرُّ فَيَـُٔوۡسٌ قَنُوۡطٌ ﴿۵۰﴾

51. Na kama Tukimwonjesha rehema Yetu baada ya dhara iliyomgusa bila shaka atasema: Hii ndiyo yangu, wala sidhani ya kwamba saa ile itatokea, na kama nikirudishwa kwa Mola wangu (haidhuru) bila shaka yako mema Kwake yaliyowekwa kwa ajili yangu. Basi Tutawajulisha wale waliokufuru hayo waliyoyatenda na kwa kweli Tutawaonjesha adhabu ngumu.

وَلَئِنۡ اَذَقۡنٰهُ رَحۡمَةً مِّنَّا مِنۡۢ بَعۡدِ ضَرَّآءَ مَسَّتۡهُ لَيَقُوۡلَنَّ هٰذَا لِىۡ ۙ وَمَاۤ اَظُنُّ السَّاعَةَ قَآئِمَةً ۙ وَّلَئِنۡ رُّجِعۡتُ اِلٰى رَبِّىۡۤ اِنَّ لِىۡ عِنۡدَهٗ لَلۡحُسۡنٰى ۚ فَلَنُنَبِّئَنَّ الَّذِيۡنَ كَفَرُوۡا بِمَا عَمِلُوۡا ۫ وَلَنُذِيۡقَنَّهُمۡ مِّنۡ عَذَابٍ غَلِيۡظٍ ﴿۵۱﴾

52. Na Tunapomneemesha mwanadamu hukengeuka na kujitenga kando, na shari inapomgusa, basi huomba sana dua.

وَاِذَاۤ اَنۡعَمۡنَا عَلَى الۡاِنۡسَانِ اَعۡرَضَ وَنَاٰ بِجَانِبِهٖ ۚ وَاِذَا مَسَّهُ الشَّرُّ فَذُوۡ دُعَآءٍ عَرِيۡضٍ ﴿۵۲﴾

Aya 48. *Saa ile.* Karibu wafasiri wote wanakubaliana ya kuwa saa inayosemwa hapa ni saa ya Kiyama. Lakini katika Kurani, *saa ile,* pia mara nyingi imesemwa kwa maana ya saa ya maangamizo ya maadui wa Mtume *s.a.w.* Basi iwe saa ya Kiyama au saa ya maangamizo ya makafiri elimu yake haijulikani na ye yote isipokuwa Allah.

قُلْ اَرَءَيْتُمْ اِنْ كَانَ مِنْ عِنْدِ اللّٰهِ ثُمَّ كَفَرْتُمْ بِهٖ مَنْ اَضَلُّ مِمَّنْ هُوَ فِيْ شِقَاقٍۭ بَعِيْدٍ ﴿٥٣﴾

53. Sema: Mwaonaje, ikiwa kama (maneno) haya yametoka kwa Allah kisha mkayakataa, ni nani aliyepotea zaidi kuliko yule aliye katika upinzani wa mbali?

سَنُرِيْهِمْ اٰيٰتِنَا فِي الْاٰفَاقِ وَفِيْٓ اَنْفُسِهِمْ حَتّٰى يَتَبَيَّنَ لَهُمْ اَنَّهُ الْحَقُّ ؕ اَوَلَمْ يَكْفِ بِرَبِّكَ اَنَّهٗ عَلٰى كُلِّ شَيْءٍ شَهِيْدٌ ﴿٥٤﴾

54. Hivi punde Tutawaonyesha Ishara Zetu zikitokea kwenye upeo wa macho na ndani ya nafsi zao mpaka iwa-bainikie kwamba hiyo ndiyo kweli. Je, haitoshi kwa Mola wako kwamba Yeye ni Msimamizi juu ya kila kitu?

اَلَآ اِنَّهُمْ فِيْ مِرْيَةٍ مِّنْ لِّقَآءِ رَبِّهِمْ ؕ اَلَآ اِنَّهٗ بِكُلِّ شَيْءٍ مُّحِيْطٌ ﴿٥٥﴾ ع

55. Jihadharini! bila shaka watu hawa wanafanya shaka katika kukutana na Mola wao. Angalieni! hakika Yeye Amekizunguka kila kitu.

Aya 54. *Aafaaqi.* Neno hili maana yake ni mipaka ya ardhi na sehemu zake za mbali.

Aya hii inaashiria ya kwamba Uislamu karibuni utaenea katika nchi za mbali na katika nchi za Waarabu wenyewe.

سُوْرَةُ الشُّوْرٰى مَكِّيَّةٌ وَّ هِيَ مَعَ الْبَسْمَلَةِ اَرْبَعٌ وَّ خَمْسُوْنَ اٰيَةً وَّ خَمْسَةُ رُكُوْعَاتٍ

42. SURA ASH-SHUURAA

Imeteremshwa Makka

Ina mafungu 5 na Aya 54 pamoja na Bismillahi

بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ ①

1. Kwa jina la Allah, Mwingi wa rehema, Mwingi wa ukarimu.

حٰمٓ ②

2. Ahimidiwaye, Atukuzwaye,

عٓسٓقٓ ③

3. Ajuaye, Asikiaye, Awezaye.

كَذٰلِكَ يُوْحِيْٓ اِلَيْكَ وَ اِلَى الَّذِيْنَ مِنْ قَبْلِكَ ۙ اللّٰهُ الْعَزِيْزُ الْحَكِيْمُ ④

4. Hivi ndivyo Allah Mwenye ushindi kamili na hekima Anavyokufunulia na (Alivyowafunulia) wale waliokutangulia.

لَهٗ مَا فِي السَّمٰوٰتِ وَمَا فِي الْاَرْضِ ؕ وَهُوَ الْعَلِيُّ الْعَظِيْمُ ⑤

5. Ni Vyake vilivyomo mbinguni na vilivyomo ardhini, na Yeye ndiye Aliye juu, Mkuu.

تَكَادُ السَّمٰوٰتُ يَتَفَطَّرْنَ مِنْ فَوْقِهِنَّ وَالْمَلٰٓئِكَةُ يُسَبِّحُوْنَ بِحَمْدِ رَبِّهِمْ وَ يَسْتَغْفِرُوْنَ لِمَنْ فِي الْاَرْضِ ؕ اَلَآ اِنَّ اللّٰهَ هُوَ الْغَفُوْرُ الرَّحِيْمُ ⑥

6. Ni karibu mbingu zipasuke toka juu yao, na Malaika hutukuza kwa kumsifu Mola wao na huwaombea msamaha waliomo ardhini. Angalieni! hakika Allah ni Msamehevu, Mwenye huruma.

Sura hii ilishuka Makka. Jina lake linatoka katika Aya 39 inayowaagiza Waislamu kufanya desturi ya kushauriana katika mambo yanye maana.

Aya 2-3. *Haa Miim 'Ain Siin Qaaf* (Ahimidiwaye, Atukuzwaye, Ajuaye, Asikiaye, Awezaye). Herufi hizi pia zinaweza kuwa na maana hizi: *Haa* ni *Haafidhul-Kitaab* (Mhifadhi wa Kitabu), *Miim* ni *Munazzilul-Kitaab* (Mteremshaji wa Kitabu); kama ambavyo katika sura hii mnaelezwa habari za kuteremshwa Kitabu cha Kurani na kukihifadhi. *'Ain* ni *'Aliyyun, 'Aliimun, 'Aziizun* (Aliye Juu, Ajuaye, Mwenye nguvu). *Siin* ni *Samii'un* (Asikiaye) na *Qaaf* ni *Qaadirun, Qahhaarun* (Mwenye kudra, Mwenye kushinda).

Aya 6. *Ni karibu mbingu zipasuke,* yaani karibu adhabu ishuke na maangamizo yatokee kwa sababu ya vitendo viovu vya wanadamu, lakini kwa sababu tatu jambo hili linacheleweshwa: (1) *Malaika hutukuza kwa kumsifu Allah;* (2) *huwaombea msamaha waliomo ardhini;* (3) *Mungu ni Msamehevu, Mwenye huruma.*

وَالَّذِيْنَ اتَّخَذُوْا مِنْ دُوْنِهٖٓ اَوْلِيَآءَ اللّٰهُ حَفِيْظٌ عَلَيْهِمْ ۗ وَمَآ اَنْتَ عَلَيْهِمْ بِوَكِيْلٍ ۝٧

7. Na wale walioshika walinzi wengine badala Yake, Allah Ndiye Mhifadhi wao, nawe si mlinzi juu yao.

وَكَذٰلِكَ اَوْحَيْنَآ اِلَيْكَ قُرْاٰنًا عَرَبِيًّا لِّتُنْذِرَ اُمَّ الْقُرٰى وَمَنْ حَوْلَهَا وَتُنْذِرَ يَوْمَ الْجَمْعِ لَا رَيْبَ فِيْهِ ۭ فَرِيْقٌ فِي الْجَنَّةِ وَفَرِيْقٌ فِي السَّعِيْرِ ۝٨

8. Na kadhalika Tumekufunulia Kurani kwa Kiarabu ili uuonye mji ulio Mama wa miji na iliyoko pembezoni mwake na ili uonye kuhusiana na siku ya Mkutano isiyo na shaka. Kundi moja litakuwa Peponi na kundi lingine litakuwa Motoni.

وَلَوْ شَاۗءَ اللّٰهُ لَجَعَلَهُمْ اُمَّةً وَّاحِدَةً وَّلٰكِنْ يُّدْخِلُ مَنْ يَّشَاۗءُ فِيْ رَحْمَتِهٖ ۭ وَالظّٰلِمُوْنَ مَا لَهُمْ مِّنْ وَّلِيٍّ وَّلَا نَصِيْرٍ ۝٩

9. Na Allah Angalipenda Angewafanya wote kundi moja, lakini Humwingiza katika rehema Yake Amtakaye, na wadhalimu hawana mlinzi wala msaidizi.

اَمِ اتَّخَذُوْا مِنْ دُوْنِهٖٓ اَوْلِيَاۗءَ ۚ فَاللّٰهُ هُوَ الْوَلِيُّ وَهُوَ يُحْيِ الْمَوْتٰى ۡ وَهُوَ عَلٰي كُلِّ شَيْءٍ قَدِيْرٌ ۝٩ ع

10. Je, wao wameshika walinzi wengine badala Yake lakini Mlinzi hasa ni Allah, na Yeye ndiye Huwahuisha waliokufa; naye ni Mwenye uwezo juu ya kila kitu.

FUNGU 2

وَمَا اخْتَلَفْتُمْ فِيْهِ مِنْ شَيْءٍ فَحُكْمُهٗٓ اِلَى اللّٰهِ ۭ ذٰلِكُمُ اللّٰهُ رَبِّيْ عَلَيْهِ تَوَكَّلْتُ ۡ وَاِلَيْهِ اُنِيْبُ ۝١١

11. Na mkihitilafiana juu ya jambo lo lote, basi hukumu yake ni kwa Allah. Huyu Ndiye Allah, Mola wangu nimtegemeaye, na Kwake naelekea.

Aya 8. Nyumba ya kwanza kabisa kuwahi kujengwa kwa shabaha ya kumwabudu Allah ni Al-kaaba iliyoko katika mji uitwao Makka. Ni mji huu unaorejewa kuwa ni *ummul-Quraa* (mama wa miji yote). Maneno haya yaweza kuashiria umuhimu wake kwa kulinganishwa na miji mingine yote au kwa tafsiri ya neno ya neno yaweza pia kuwa na maana ya mji wa kwanza kabisa kupata kujengwa. Kama ichukuliwe nadharia hiyo ya pili, itakuwa imedokezwa kwamba katika zama za kale, mahali pale pale ulipo mji wa Makka, mji ulikua pole pole pembezoni mwa nyumba ya Mungu ilipokuwa imejengwa kwa mara ya kwanza na watu wasiojulikana. Wanadamu walijifunza kujenga miji kwa kuuigiza mji huu. Hivyo basi waweza kurejewa kuwa ndio mama wa miji yote.

فَاطِرُ السَّمٰوٰتِ وَالْاَرْضِ ؕ جَعَلَ لَكُمْ
مِّنْ اَنْفُسِكُمْ اَزْوَاجًا وَّمِنَ الْاَنْعَامِ
اَزْوَاجًا ۚ يَذْرَؤُكُمْ فِيْهِ ؕ لَيْسَ كَمِثْلِهٖ
شَيْءٌ ۚ وَهُوَ السَّمِيْعُ الْبَصِيْرُ ﴿١٢﴾

12. Muumba wa mbingu na ardhi. Amewafanyieni wenzi katika jinsi yenu na wenza kwa wanyama (pia). Huwazidisheni kwa njia hii; hakuna cho chote mfano Wake; Naye ni Mwenye kusikia, Mwenye kuona.

لَهٗ مَقَالِيْدُ السَّمٰوٰتِ وَالْاَرْضِ ۚ يَبْسُطُ
الرِّزْقَ لِمَنْ يَّشَآءُ وَيَقْدِرُ ؕ اِنَّهٗ بِكُلِّ
شَيْءٍ عَلِيْمٌ ﴿١٣﴾

13. Funguo za mbingu na ardhi zi Kwake, Humfungulia riziki Amtakaye na Humdhikisha; bila shaka Yeye ndiye Ajuaye kila kitu.

شَرَعَ لَكُمْ مِّنَ الدِّيْنِ مَا وَصّٰى بِهٖ نُوْحًا
وَّالَّذِيْٓ اَوْحَيْنَآ اِلَيْكَ وَمَا وَصَّيْنَا بِهٖٓ
اِبْرٰهِيْمَ وَمُوْسٰى وَعِيْسٰٓى اَنْ اَقِيْمُوا
الدِّيْنَ وَلَا تَتَفَرَّقُوْا فِيْهِ ؕ كَبُرَ عَلَى
الْمُشْرِكِيْنَ مَا تَدْعُوْهُمْ اِلَيْهِ ؕ اَللّٰهُ
يَجْتَبِيْٓ اِلَيْهِ مَنْ يَّشَآءُ وَيَهْدِيْٓ اِلَيْهِ
مَنْ يُّنِيْبُ ﴿١٤﴾

14. Amewapeni sheria ya dini Aliyomwusia Nuhu na Tuliyokufunulia wewe na Tuliyowausia Ibrahimu na Musa na Isa kwamba simamisheni dini wala msifarakiane kwayo; ni ngumu kwa washirikina (dini ile) unayowaitia; Allah Humchagua Kwake Amtakaye na Humwongoza Kwake aelekeaye.

وَمَا تَفَرَّقُوْٓا اِلَّا مِنْۢ بَعْدِ مَا جَآءَهُمُ
الْعِلْمُ بَغْيًۢا بَيْنَهُمْ ؕ وَلَوْلَا كَلِمَةٌ سَبَقَتْ
مِنْ رَّبِّكَ اِلٰٓى اَجَلٍ مُّسَمًّى لَّقُضِيَ
بَيْنَهُمْ ؕ وَاِنَّ الَّذِيْنَ اُوْرِثُوا الْكِتٰبَ مِنْۢ
بَعْدِهِمْ لَفِيْ شَكٍّ مِّنْهُ مُرِيْبٍ ﴿١٥﴾

15. Hawakuhitilafiana ila baada ya kuwafikia elimu kwa sababu ya uasi baina yao; na kama isingalikuwa kauli iliyotangulia kutoka kwa Mola wako, juu ya muda uliowekwa, hukumu ingalitolewa baina yao. Na kwa yakini wale waliorithishwa Kitabu baada yao wanakionea shaka ihangaishayo.

فَلِذٰلِكَ فَادْعُ ۚ وَاسْتَقِمْ كَمَآ اُمِرْتَ ۚ
وَلَا تَتَّبِعْ اَهْوَآءَهُمْ ۚ وَقُلْ اٰمَنْتُ بِمَآ
اَنْزَلَ اللّٰهُ مِنْ كِتٰبٍ ۚ وَاُمِرْتُ لِاَعْدِلَ
بَيْنَكُمْ ؕ اَللّٰهُ رَبُّنَا وَرَبُّكُمْ ؕ لَنَآ اَعْمَالُنَا

16. Kwa ajili ya hayo waite, na ukaendelee kwa kudumu kama unavyoamriwa, wala usifuate matamanio yao; na useme: Naamini Aliyoyateremsha Allah Kitabuni, na nimeamrishwa nifanye uadilifu baina yenu, Allah Ndiye Mola wangu na

وَلَكُمْ اَعْمَالُكُمْ ؕ لَا حُجَّةَ بَيْنَنَا وَبَيْنَكُمْ ؕ اَللّٰهُ يَجْمَعُ بَيْنَنَا ۚ وَاِلَيْهِ الْمَصِيْرُ ﴿١٦﴾

pia ni Mola wenu, vitendo vyetu ni kwa ajili yetu, na vitendo vyenu kwa ajili yenu: hakuna ugomvi baina yetu na yenu, Allah Atatukusanya pamoja, na marejeo ni Kwake.

وَالَّذِيْنَ يُحَآجُّوْنَ فِى اللّٰهِ مِنْۢ بَعْدِ مَا اسْتُجِيْبَ لَهٗ حُجَّتُهُمْ دَاحِضَةٌ عِنْدَ رَبِّهِمْ وَعَلَيْهِمْ غَضَبٌ وَّلَهُمْ عَذَابٌ شَدِيْدٌ ﴿١٧﴾

17. Na wale wanaohojiana juu ya Allah baada ya kumkubali, hoja yao imebatilika mbele ya Mola wao, na juu yao iko ghadhabu na itakuwa kwao adhabu kali.

اَللّٰهُ الَّذِىْۤ اَنْزَلَ الْكِتٰبَ بِالْحَقِّ وَالْمِيْزَانَ ؕ وَمَا يُدْرِيْكَ لَعَلَّ السَّاعَةَ قَرِيْبٌ ﴿١٨﴾

18. Allah Ndiye Aliyeteremsha Kitabu kwa haki na mizani. Na ni nini kitakujulisha ya kwamba labda saa ile imekaribia.

يَسْتَعْجِلُ بِهَا الَّذِيْنَ لَا يُؤْمِنُوْنَ بِهَا ۚ وَالَّذِيْنَ اٰمَنُوْا مُشْفِقُوْنَ مِنْهَا ۙ وَيَعْلَمُوْنَ اَنَّهَا الْحَقُّ ؕ اَلَاۤ اِنَّ الَّذِيْنَ يُمَارُوْنَ فِى السَّاعَةِ لَفِىْ ضَلٰلٍۢ بَعِيْدٍ ﴿١٩﴾

19. Wasioamini (saa ile) huiomba ifike upesi, lakini wanaoiamini wanaiogopa na wanatambua kwamba matokeo yake ni haki. Jihadharini! Kwa hakika hao wanaobishana katika habari ya saa hiyo wamo katika upotevu wa mbali.

اَللّٰهُ لَطِيْفٌۢ بِعِبَادِهٖ يَرْزُقُ مَنْ يَّشَآءُ ۚ وَهُوَ الْقَوِىُّ الْعَزِيْزُ ﴿٢٠﴾ ع ٣

20. Allah ni Mpole kwa watumishi Wake. Humpa riziki Amtakaye, naye ni Mwenye nguvu, Mwenye ushindi kamili.

FUNGU 3

مَنْ كَانَ يُرِيْدُ حَرْثَ الْاٰخِرَةِ نَزِدْ لَهٗ فِىْ حَرْثِهٖ ۚ وَمَنْ كَانَ يُرِيْدُ حَرْثَ الدُّنْيَا نُؤْتِهٖ مِنْهَا وَمَا لَهٗ فِى الْاٰخِرَةِ مِنْ نَّصِيْبٍ ﴿٢١﴾

21. Mwenye kutaka mavuno ya Akhera Tutamzidishia katika mavuno yake; na anayetaka mavuno ya dunia Tutampayo, lakini Akhera hana sehemu yo yote.

اَمْ لَهُمْ شُرَكٰٓؤُا شَرَعُوْا لَهُمْ مِّنَ الدِّيْنِ مَا لَمْ يَاْذَنْۢ بِهِ اللّٰهُ ؕ وَلَوْلَا كَلِمَةُ الْفَصْلِ لَقُضِىَ بَيْنَهُمْ ؕ وَاِنَّ الظّٰلِمِيْنَ لَهُمْ عَذَابٌ اَلِيْمٌ ﴿٢٢﴾

22. Je, wana washirika waliowawekea dini Asiyoitolea Allah idhini Yake? Na kama lisingalikuwako neno la kupambanua, hukumu ingalikatwa baina yao; na kwa yakini itakuwa kwa wadhalimu adhabu iumizayo.

تَرَى الظّٰلِمِيْنَ مُشْفِقِيْنَ مِمَّا كَسَبُوْا وَهُوَ وَاقِعٌۢ بِهِمْ ؕ وَالَّذِيْنَ اٰمَنُوْا وَعَمِلُوا الصّٰلِحٰتِ فِيْ رَوْضٰتِ الْجَنّٰتِ ۚ لَهُمْ مَّا يَشَآءُوْنَ عِنْدَ رَبِّهِمْ ؕ ذٰلِكَ هُوَ الْفَضْلُ الْكَبِيْرُ ﴿٢٢﴾

23. Utawaona wadhalimu wakiogopa kwa sababu ya yale waliyoyachuma, nayo yatawatokea; na wale walioamini na kutenda wema watakuwamo katika mabustani ya Peponi; watapata watakayoyataka kwa Mola wao. Hiyo ndiyo fadhili kubwa.

ذٰلِكَ الَّذِيْ يُبَشِّرُ اللّٰهُ عِبَادَهُ الَّذِيْنَ اٰمَنُوْا وَعَمِلُوا الصّٰلِحٰتِ ؕ قُلْ لَّاۤ اَسْـَٔلُكُمْ عَلَيْهِ اَجْرًا اِلَّا الْمَوَدَّةَ فِي الْقُرْبٰى ؕ وَمَنْ يَّقْتَرِفْ حَسَنَةً نَّزِدْ لَهٗ فِيْهَا حُسْنًا ؕ اِنَّ اللّٰهَ غَفُوْرٌ شَكُوْرٌ ﴿٢٣﴾

24. Hii ndiyo habari nzuri ambayo Allah Huwaambia watumishi Wake walioamini na kufanya vitendo vizuri. Sema: Kwa hilo siombi ujira wo wote kutoka kwenu isipokuwa tu mpendane kama ndugu. Na ye yote afanyaye kitendo cha wema tunamuongezea zaidi uzuri wa wema wake, kwa hakika Allah ni Msamehevu, Mwenye shukurani.

اَمْ يَقُوْلُوْنَ افْتَرٰى عَلَى اللّٰهِ كَذِبًا ۚ فَاِنْ يَّشَاِ اللّٰهُ يَخْتِمْ عَلٰى قَلْبِكَ ؕ وَيَمْحُ اللّٰهُ الْبَاطِلَ وَيُحِقُّ الْحَقَّ بِكَلِمٰتِهٖ ؕ اِنَّهٗ عَلِيْمٌۢ بِذَاتِ الصُّدُوْرِ ﴿٢٤﴾

25. Au wanasema: Amemzulia Allah uwongo? Kama Allah Angalipenda Angalipiga muhuri moyoni mwako. Na Allah Hufuta uwongo na kustawisha ukweli kwa maneno Yake. Bila shaka Yeye Anayajua vizuri sana yaliyomo vifuani.

وَهُوَ الَّذِيْ يَقْبَلُ التَّوْبَةَ عَنْ عِبَادِهٖ وَيَعْفُوْا عَنِ السَّيِّاٰتِ وَيَعْلَمُ مَا تَفْعَلُوْنَ ﴿٢٥﴾

26. Naye ndiye Anayepokea toba za watu Wake, na Husamehe makosa, na Huyajua mnayoyatenda.

Aya 24. *Ila mapenzi katika ndugu.* Baadhi ya mufasirina wametafsiri maneno haya hivi: Siombi malipo yo yote kwenu ila *wapendwe karibu zangu.*" Tafsiri hii si nzuri na imekataliwa na Ibni Abbas (Bukhari). Maana zake zinaweza kuwa hizi: (1) siombi malipo kwenu ila mnipende kwa vile mimi ni ndugu yenu; (2) siombi malipo kwenu ila muwe na mapenzi kwa ndugu zenu; (3) siombi malipo kwenu ila muwe na mapenzi ya vitendo vinavyokaribishwa kwa Allah. Hii ya tatu ndiyo maana iliyo nzuri zaidi na inapatana na maneno ya Aya za mbele na nyuma. (4) Pia maana yake inaweza kuwa. Mimi siombi ujira kwenu ila ni mapenzi ya udugu niliyo nayo kwenu ndiyo yananifanya niwahubirieni habari hizi mara kwa mara.

27. Na Huwajibu wanaoamini na kutenda wema na Huwazidishia fadhili Zake, na makafiri wana adhabu kali.

وَيَسْتَجِيْبُ الَّذِيْنَ اٰمَنُوْا وَعَمِلُوا الصّٰلِحٰتِ وَيَزِيْدُهُمْ مِّنْ فَضْلِهٖ ؕ وَالْكٰفِرُوْنَ لَهُمْ عَذَابٌ شَدِيْدٌ ﴿٢٧﴾

28. Na kama Allah Angetoa riziki nyingi kwa watumishi Wake bila shaka wangaliasi ardhini, lakini Huiteremsha kwa kipimo Akipendacho. Hakika Yeye kwa watumishi Wake ni Mwenye habari, Mwenye kuona.

وَلَوْ بَسَطَ اللّٰهُ الرِّزْقَ لِعِبَادِهٖ لَبَغَوْا فِي الْاَرْضِ وَلٰكِنْ يُّنَزِّلُ بِقَدَرٍ مَّا يَشَآءُ ؕ اِنَّهٗ بِعِبَادِهٖ خَبِيْرٌۢ بَصِيْرٌ ﴿٢٨﴾

29. Naye ndiye Huiteremsha mvua baada ya wao kukata tamaa na Hueneza rehema Yake; naye ndiye Mlinzi, Ahimidiwaye.

وَهُوَ الَّذِيْ يُنَزِّلُ الْغَيْثَ مِنْۢ بَعْدِ مَا قَنَطُوْا وَيَنْشُرُ رَحْمَتَهٗ ؕ وَهُوَ الْوَلِيُّ الْحَمِيْدُ ﴿٢٩﴾

30. Na katika Ishara Zake ni kuumbwa mbingu na ardhi na Alivyovieneza humo katika vyenye uhai; tena ndiye Mwenye uwezo wa kuvikusanya Apendapo.

وَمِنْ اٰيٰتِهٖ خَلْقُ السَّمٰوٰتِ وَالْاَرْضِ وَمَا بَثَّ فِيْهِمَا مِنْ دَآبَّةٍ ؕ وَهُوَ عَلٰى جَمْعِهِمْ اِذَا يَشَآءُ قَدِيْرٌ ﴿٣٠﴾

FUNGU 4

31. Na msiba unaowapateni unatokana na yale iliyoyachuma mikono yenu, wakati Yeye Husamehe mengi.

وَمَآ اَصَابَكُمْ مِّنْ مُّصِيْبَةٍ فَبِمَا كَسَبَتْ اَيْدِيْكُمْ وَيَعْفُوْا عَنْ كَثِيْرٍ ﴿٣٠﴾

32. Na ninyi hamwezi kudhoofisha ardhini, na pasipo Allah ninyi hamna mlinzi wala msaidizi.

وَمَآ اَنْتُمْ بِمُعْجِزِيْنَ فِي الْاَرْضِ ۖ وَمَا لَكُمْ مِّنْ دُوْنِ اللّٰهِ مِنْ وَّلِيٍّ وَّلَا نَصِيْرٍ ﴿٣٢﴾

33. Na katika Ishara Zake ni majahazi baharini yaliyo kama milima.

وَمِنْ اٰيٰتِهِ الْجَوَارِ فِي الْبَحْرِ كَالْاَعْلَامِ ﴿٣٣﴾

34. Kama Akitaka Hutuliza upepo, nayo husimama tu juu yake (bahari), kwa yakini katika hayo ziko Ishara kwa kila afanyaye subira, anayeshukuru.

اِنْ يَّشَاْ يُسْكِنِ الرِّيْحَ فَيَظْلَلْنَ رَوَاكِدَ عَلٰى ظَهْرِهٖ ؕ اِنَّ فِيْ ذٰلِكَ لَاٰيٰتٍ لِّكُلِّ صَبَّارٍ شَكُوْرٍ ﴿٣٤﴾

35. Au Huziangamiza (merikebu) kwa sababu ya yale waliyoyatenda (hao wasafiri) na Husamehe (mambo) mengi.

اَوْ يُوْبِقْهُنَّ بِمَا كَسَبُوْا وَيَعْفُ عَنْ كَثِيْرٍ ﴿٣٥﴾

36. Na watajua wale wanaojadiliana katika Ishara Zetu (ya kwamba) hawana mahali pa kukimbilia.

وَّيَعْلَمَ الَّذِيْنَ يُجَادِلُوْنَ فِيْٓ اٰيٰتِنَا ؕ مَا لَهُمْ مِّنْ مَّحِيْصٍ ﴿٣٦﴾

فَمَآ اُوْتِيْتُمْ مِّنْ شَيْءٍ فَمَتَاعُ الْحَيٰوةِ الدُّنْيَا ۚ وَمَا عِنْدَ اللّٰهِ خَيْرٌ وَّاَبْقٰى لِلَّذِيْنَ اٰمَنُوْا وَعَلٰى رَبِّهِمْ يَتَوَكَّلُوْنَ ۚ﴿٣٧﴾

37. Basi cho chote mnachopewa ni posho ya maisha ya dunia; lakini kilichoko kwa Allah ni bora na hudumu zaidi kwa wale walioamini na kumtegemea Mola wao.

وَالَّذِيْنَ يَجْتَنِبُوْنَ كَبٰٓئِرَ الْاِثْمِ وَالْفَوَاحِشَ وَاِذَا مَا غَضِبُوْا هُمْ يَغْفِرُوْنَ ۚ﴿٣٨﴾

38. Na wale wajiepushao na madhambi makubwa na mambo ya aibu na wanapokasirika wao husamehe.

وَالَّذِيْنَ اسْتَجَابُوْا لِرَبِّهِمْ وَاَقَامُوا الصَّلٰوةَ ۪ وَاَمْرُهُمْ شُوْرٰى بَيْنَهُمْ ۪ وَمِمَّا رَزَقْنٰهُمْ يُنْفِقُوْنَ ۚ﴿٣٩﴾

39. Na wale waliomwitikia Mola wao na kusimamisha Sala, na utendaji wao hufanyika kwa kushauriana wao kwa wao, na hutoa katika yale Tuliyowaruzuku.

وَالَّذِيْنَ اِذَآ اَصَابَهُمُ الْبَغْيُ هُمْ يَنْتَصِرُوْنَ ﴿٤٠﴾

40. Na wale ambao wanapodhulumiwa wao hulipa kisasi.

وَجَزٰٓؤُا سَيِّئَةٍ سَيِّئَةٌ مِّثْلُهَا ۚ فَمَنْ عَفَا وَاَصْلَحَ فَاَجْرُهٗ عَلَى اللّٰهِ ؕ اِنَّهٗ لَا يُحِبُّ الظّٰلِمِيْنَ ﴿٤١﴾

41. Na malipo ya ubaya ni ubaya ulio sawa nao; lakini anayesamehe kwa nia ya kusuluhisha, basi ujira wake ni juu ya Allah; bila shaka Yeye Hawapendi wadhalimu.

وَلَمَنِ انْتَصَرَ بَعْدَ ظُلْمِهٖ فَاُولٰٓئِكَ مَا عَلَيْهِمْ مِّنْ سَبِيْلٍ ؕ﴿٤٢﴾

42. Naye ajilipizaye baada ya kudhulumiwa, basi hawa ndio juu yao hakuna lawama.

اِنَّمَا السَّبِيْلُ عَلَى الَّذِيْنَ يَظْلِمُوْنَ النَّاسَ وَيَبْغُوْنَ فِى الْاَرْضِ بِغَيْرِ الْحَقِّ ؕ اُولٰٓئِكَ لَهُمْ عَذَابٌ اَلِيْمٌ ﴿٤٣﴾

43. Lawama iko tu juu ya wale wanaowadhulumu watu na huasi ardhini pasipo haki: hao ndio watakaopata adhabu iumizayo.

وَلَمَنْ صَبَرَ وَغَفَرَ اِنَّ ذٰلِكَ لَمِنْ عَزْمِ الْاُمُوْرِ ۚ﴿٤٤﴾

44. Na anayesubiri na kusamehe; bila shaka hilo ni katika mambo thabiti.

FUNGU 5

وَمَنْ يُّضْلِلِ اللّٰهُ فَمَا لَهٗ مِنْ وَّلِيٍّ مِّنْۢ بَعْدِهٖ ؕ وَتَرَى الظّٰلِمِيْنَ لَمَّا رَاَوُا الْعَذَابَ يَقُوْلُوْنَ هَلْ اِلٰى مَرَدٍّ مِّنْ سَبِيْلٍ ۚ﴿٤٥﴾

45. Na ambaye Allah Anamwacha kupotea, basi hana mlinzi baada Yake. Na utawaona wadhalimu watakapoiona adhabu, watasema: Je, iko njia ya kuiepuka?

Aya 39. *Sheria yao ni kushauriana wao kwa wao.* Desturi ya waaminio ni kushauriana

وَتَرٰىهُمْ يُعْرَضُوْنَ عَلَيْهَا خٰشِعِيْنَ مِنَ الذُّلِّ يَنْظُرُوْنَ مِنْ طَرْفٍ خَفِيٍّ ؕ وَقَالَ الَّذِيْنَ اٰمَنُوْٓا اِنَّ الْخٰسِرِيْنَ الَّذِيْنَ خَسِرُوْٓا اَنْفُسَهُمْ وَاَهْلِيْهِمْ يَوْمَ الْقِيٰمَةِ ؕ اَلَآ اِنَّ الظّٰلِمِيْنَ فِيْ عَذَابٍ مُّقِيْمٍ ﴿٤٥﴾

46. Na utawaona wakipelekwa mbele ya (adhabu) hiyo wakinyenyekea kutokana na fedheha wakitazama kwa kuinamia chini. Na walioamini watasema: Kwa hakika wenye hasara ni wale waliohasirisha nafsi zao na ahali zao siku ya Kiyama. Jihadharini! Bila shaka wadhalimu watakuwa katika adhabu inayoendelea.

وَمَا كَانَ لَهُمْ مِّنْ اَوْلِيَآءَ يَنْصُرُوْنَهُمْ مِّنْ دُوْنِ اللّٰهِ ؕ وَمَنْ يُّضْلِلِ اللّٰهُ فَمَا لَهٗ مِنْ سَبِيْلٍ ﴿٤٦﴾

47. Wala hawatakuwa na marafiki wa kuwasaidia kinyume cha Allah. Na ambaye Allah Anamwacha kupotea, basi hana njia yo yote.

اِسْتَجِيْبُوْا لِرَبِّكُمْ مِّنْ قَبْلِ اَنْ يَّاْتِيَ يَوْمٌ لَّا مَرَدَّ لَهٗ مِنَ اللّٰهِ ؕ مَا لَكُمْ مِّنْ مَّلْجَاٍ يَّوْمَئِذٍ وَّمَا لَكُمْ مِّنْ نَّكِيْرٍ ﴿٤٧﴾

48. Mwitikieni Mola wenu kabla ya kufika siku isiyoepukika itokayo kwa Allah, siku hiyo hamtakuwa na pa kukimbilia wala hamtakuwa na fursa yoyote ya kukataa.

فَاِنْ اَعْرَضُوْا فَمَآ اَرْسَلْنٰكَ عَلَيْهِمْ حَفِيْظًا ؕ اِنْ عَلَيْكَ اِلَّا الْبَلٰغُ ؕ وَاِنَّآ اِذَآ اَذَقْنَا الْاِنْسَانَ مِنَّا رَحْمَةً فَرِحَ بِهَا ۚ وَاِنْ تُصِبْهُمْ سَيِّئَةٌ ۢ بِمَا قَدَّمَتْ اَيْدِيْهِمْ فَاِنَّ الْاِنْسَانَ كَفُوْرٌ ﴿٤٨﴾

49. Na kama wakigeuka, basi Hatukukupeleka uwe mhifadhi wao, si juu yako ila kufikisha. Na kwa yakini Tunapomwonjesha mwanadamu rehema kutoka Kwetu huifurahia, na kama ikiwafikia dhara kwa sababu ya yale iliyoyatanguliza mikono yao, basi (hapo) kwa hakika mwanadamu huthibitika kuwa asiye na shukrani hata kidogo.

لِلّٰهِ مُلْكُ السَّمٰوٰتِ وَالْاَرْضِ ؕ يَخْلُقُ مَا يَشَآءُ ؕ يَهَبُ لِمَنْ يَّشَآءُ اِنَاثًا وَّيَهَبُ لِمَنْ يَّشَآءُ الذُّكُوْرَ ﴿٤٩﴾

50. Ufalme wa mbingu na ardhi ni wa Allah: Hukiumba Akipendacho, Humpa Amtakaye watoto wa kike na Humpa Amtakaye watoto wa kiume.

---

juu ya mambo yao yanayowahusu. Linapokuwa ni jambo la jamii, basi hukumu inayotolewa na Mtume wa Mungu au Khalifa wake baada ya kushauriana ndiyo inayofuatwa, hata kama hukumu hiyo iwe kinyume na vile walivyotaka watu.

Aya 50. Waarabu waliona kuzaa watoto wa kike ni jambo la fedheha (sura 16:59, 60).

اَوْ يُزَوِّجُهُمْ ذُكْرَانًا وَّاِنَاثًا ۚ وَيَجْعَلُ مَنْ يَّشَآءُ عَقِيْمًا ۭ اِنَّهٗ عَلِيْمٌ قَدِيْرٌ ۝۵۰

51. Na pengine Huwachanganya (watoto) wa kiume na wa kike na Humfanya tasa Amtakaye; hakika Yeye ni Ajuaye, Awezaye.

وَمَا كَانَ لِبَشَرٍ اَنْ يُّكَلِّمَهُ اللّٰهُ اِلَّا وَحْيًا اَوْ مِنْ وَّرَاۗئِ حِجَابٍ اَوْ يُرْسِلَ رَسُوْلًا فَيُوْحِيَ بِاِذْنِهٖ مَا يَشَاۗءُ ۭ اِنَّهٗ عَلِيٌّ حَكِيْمٌ ۝۵۱

52. Na haikuwa kwa mtu ya kwamba Allah Aseme naye ila kwa ufunuo au kwa nyuma ya pazia au Humtuma Mjumbe naye huteremsha wahyi kwa idhini Yake (wa yale) Ayapendayo (Allah); bila shaka Yeye ni mwenye shani ya juu kabisa, Mwenye hekima.

وَكَذٰلِكَ اَوْحَيْنَآ اِلَيْكَ رُوْحًا مِّنْ اَمْرِنَا ۭ مَا كُنْتَ تَدْرِيْ مَا الْكِتٰبُ وَلَا الْاِيْمَانُ وَلٰكِنْ جَعَلْنٰهُ نُوْرًا نَّهْدِيْ بِهٖ مَنْ نَّشَاۗءُ مِنْ عِبَادِنَا ۭ وَاِنَّكَ لَتَهْدِيْٓ اِلٰى صِرَاطٍ مُّسْتَقِيْمٍ ۝۵۲ۙ

53. Na kadhalika Tumekufunulia wahyi wa maneno yenye kuhuisha kwa amri Yetu, ulikuwa hujui Kitabu ni nini wala imani, lakini Tuliufanya nuru, ambayo kwayo Twamwongoza Tumtakaye katika watumishi Wetu; na kwa yakini wewe unaongoza kwenye njia iliyonyoka:

صِرَاطِ اللّٰهِ الَّذِيْ لَهٗ مَا فِي السَّمٰوٰتِ وَمَا فِي الْاَرْضِ ۭ اَلَآ اِلَى اللّٰهِ تَصِيْرُ الْاُمُوْرُ ۝۵۳ۧ

54. Njia ya Allah Ambaye ni Vyake vilivyomo mbinguni na ardhini. Jueni! mambo yote yanarudi kwa Allah.

Lakini toka mwanzo dini ya Kiislamu ilisimamisha heshima ya wanawake na ikafuta kabisa desturi ya kuwadharau. Katika Aya hii watoto wa kike wametajwa mbele kuliko wa kiume kuonyesha ya kwamba kupata watoto wa kike pia ni fadhili kubwa ya Allah.

Aya 52. Allah husema na watu wema kwa njia tatu:-

(1) *Wahyi (ufunuo)*: yaani (a) *njozi.* Kitu kinaonyeshwa ili kiwe ishara ya kitu kisichoonekana. Mathalan maziwa huonyeshwa katika ndoto kwa kutambulisha elimu, na nyati, ugonjwa; (b) *kashfi.* Njozi inayofanyika wakati mtu yu macho kabisa, yumo katika shughuli zake na anaruhusiwa kufanya mazungumzo ya kiroho na watu waliokufa; au anaonyeshwa matokeo fulani yanayotokea mahali pa mbali n.k.w. Imesemwa katika Bukhari kuwa njozi za Manabii ni wahyi.

(2) *Nyuma ya pazia.* Ni ufunuo unaoletwa kwa maneno na Allah anasema na mtu kwa namna ile ile mtu anavyozungumza na mtu mwingine, na anasikia sauti sawa na ile inayotolewa na mazungumzo ya watu, na namna hii maneno ya ufunuo yanapitishwa masikioni mwake au yanawekwa mbele yake katika maandishi na anayakariri. (Soma "Uislamu Sahihi").

(3) *Humtuma Mjumbe.* Yaani anatumwa Malaika kufikisha ujumbe kama alivyoleta Malaika Jibril maneno ya Kurani kwa Mtume *s.a.w.* na kumsomea akimfundisha.

Aya 53. *Wahyi,* yaani Kurani.

سُوْرَةُ الزُّخْرُفِ مَكِّيَّةٌ وَّ هِيَ مَعَ الْبَسْمَلَةِ تِسْعُوْنَ اٰيَةً وَّ سَبْعَةُ رُكُوْعَاتٍ

43. SURA AZ-ZUKHRUF

Imeteremshwa Makka

Ina mafungu 7 na Aya 90 pamoja na Bismillahi

بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ ﴿١﴾

1. Kwa jina la Allah, Mwingi wa rehema, Mwingi wa ukarimu.

حٰمٓ ﴿٢﴾

2. Ahimidiwaye, Atukuzwaye.

وَالْكِتٰبِ الْمُبِيْنِ ﴿٣﴾

3. Naapa kwa Kitabu kinachobainisha

معانقة ١١ عند المتقدمين

اِنَّا جَعَلْنٰهُ قُرْءٰنًا عَرَبِيًّا لَّعَلَّكُمْ تَعْقِلُوْنَ ﴿٤﴾

4. Bila shaka Tumeifanya Kurani iliyo fasaha ili mfahamu.

وَاِنَّهٗ فِيْٓ اُمِّ الْكِتٰبِ لَدَيْنَا لَعَلِيٌّ حَكِيْمٌ ﴿٥﴾

5. Na kwa yakini (Kurani) hii imo ndani ya mama wa kitabu. Bila shaka kwetu (Kurani hii) ni yenye shani ya hali ya juu na yenye hekima.

اَفَنَضْرِبُ عَنْكُمُ الذِّكْرَ صَفْحًا اَنْ كُنْتُمْ قَوْمًا مُّسْرِفِيْنَ ﴿٦﴾

6. Je, Tutaacha kuwakumbusheni kwa sababu mmekuwa watu mliopita kiasi?

وَكَمْ اَرْسَلْنَا مِنْ نَّبِيٍّ فِي الْاَوَّلِيْنَ ﴿٧﴾

7. Na Tuliwapeleka Manabii wangapi katika watu wa zamani?

وَمَا يَاْتِيْهِمْ مِّنْ نَّبِيٍّ اِلَّا كَانُوْا بِهٖ يَسْتَهْزِءُوْنَ ﴿٨﴾

8. Na hakuwafikia Nabii ye yote ila walikuwa wakimfanyia mzaha.

فَاَهْلَكْنَآ اَشَدَّ مِنْهُمْ بَطْشًا وَّمَضٰى مَثَلُ الْاَوَّلِيْنَ ﴿٩﴾

9. Basi Tuliwaangamiza waliokuwa na nguvu zaidi kuliko hao, na mfano wa watu wa zamani umekwisha pita.

وَلَئِنْ سَاَلْتَهُمْ مَّنْ خَلَقَ السَّمٰوٰتِ وَالْاَرْضَ لَيَقُوْلُنَّ خَلَقَهُنَّ الْعَزِيْزُ الْعَلِيْمُ ﴿١٠﴾

10. Na ukiwauliza: Ni nani ameziumba mbingu na ardhi? Kwa yakini watasema: Ameziumba Mwenye ushindi kamili, Ajuaye.

الَّذِيْ جَعَلَ لَكُمُ الْاَرْضَ مَهْدًا وَّجَعَلَ لَكُمْ فِيْهَا سُبُلًا لَّعَلَّكُمْ تَهْتَدُوْنَ ﴿١١﴾

11. Ambaye amewafanyieni ardhi kuwa tandiko, na Akawafanyieni njia ndani yake ili mwongoke.

Sura hii ilishuka Makka, na imepewa jina toka Aya 36.

Aya 2. *Haa Miim* (Tazama sura zilizopita.

Aya 5. Maneno *umul-Kitaab* kwa kawaida hutumika mintarafu ya sura ya ufunguzi ya Kurani, *Alfaatiha* ambayo ikiwa kama mbegu inayo mafundisho yote ya msingi na sifa zote asilia za Kurani.

وَالَّذِیْ نَزَّلَ مِنَ السَّمَآءِ مَآءًۢ بِقَدَرٍ ۚ فَاَنْشَرْنَا بِهٖ بَلْدَةً مَّیْتًا ۚ كَذٰلِكَ تُخْرَجُوْنَ ﴿۱۱﴾

12. Na Ambaye ameteremsha maji mawinguni kwa makadirio, na kwayo Tukaufufua mji uliokufa, ndivyo mtakavyotolewa.

وَالَّذِیْ خَلَقَ الْاَزْوَاجَ كُلَّهَا وَجَعَلَ لَكُمْ مِّنَ الْفُلْكِ وَالْاَنْعَامِ مَا تَرْكَبُوْنَ ﴿۱۲﴾

13. Na Ambaye Ameumba jozi za kila namna na Akawafanyieni merikebu na wanyama mnaowapanda.

لِتَسْتَوٗا عَلٰى ظُهُوْرِهٖ ثُمَّ تَذْكُرُوْا نِعْمَةَ رَبِّكُمْ اِذَا اسْتَوَیْتُمْ عَلَیْهِ وَتَقُوْلُوْا سُبْحٰنَ الَّذِیْ سَخَّرَ لَنَا هٰذَا وَمَا كُنَّا لَهٗ مُقْرِنِیْنَ ﴿۱۳﴾

14. Ili mkae migongoni mwao kisha mkumbuke neema za Mola wenu mnapokaa sawasawa juu yao na mseme: Atukuzwe Yeye Aliyetutiishia haya na tusingeliweza kutenda haya wenyewe.

وَاِنَّاۤ اِلٰى رَبِّنَا لَمُنْقَلِبُوْنَ ﴿۱۴﴾

15. Na bila shaka sisi tunarudia kwa Mola wetu.

وَجَعَلُوْا لَهٗ مِنْ عِبَادِهٖ جُزْءًا ؕ اِنَّ الْاِنْسَانَ لَكَفُوْرٌ مُّبِیْنٌ ﴿۱۵﴾

16. Na walimfanyia baadhi ya watumishi Wake kuwa sehemu ya dhati Yake. Kwa hakika mwanadamu ni mtovu waziwazi wa shukurani.

FUNFU 2

اَمِ اتَّخَذَ مِمَّا یَخْلُقُ بَنٰتٍ وَّاَصْفٰىكُمْ بِالْبَنِیْنَ ﴿۱۶﴾

17. Je, Amejichukulia binti katika vile Alivyoviumba na kukuchagulieni ninyi watoto wanaume?

وَاِذَا بُشِّرَ اَحَدُهُمْ بِمَا ضَرَبَ لِلرَّحْمٰنِ مَثَلًا ظَلَّ وَجْهُهٗ مُسْوَدًّا وَّهُوَ كَظِیْمٌ ﴿۱۷﴾

18. Na anapoambiwa mmoja wao yale Aliyompigia mfano Rahman, uso wake huwa mweusi (husinyaa) akijitahidi sana kuificha huzuni yake.

اَوَمَنْ یُّنَشَّؤُا فِی الْحِلْیَةِ وَهُوَ فِی الْخِصَامِ غَیْرُ مُبِیْنٍ ﴿۱۸﴾

19. Je, aliyelelewa katika mapambo naye katika mabishano hawezi kusema bayana!

وَجَعَلُوا الْمَلٰٓئِكَةَ الَّذِیْنَ هُمْ عِبٰدُ الرَّحْمٰنِ اِنَاثًا ؕ اَشَهِدُوْا خَلْقَهُمْ ؕ سَتُكْتَبُ شَهَادَتُهُمْ وَیُسْـَٔلُوْنَ ﴿۱۹﴾

20. Na wanawafanya Malaika, ambao ni Watumishi wa Rahmani, kuwa wanawake. Je, wameshuhudia kuumbwa kwao? Ushahidi wao utaandikwa na wataulizwa.

Lakini hapa yaelekea yametumika mintarafu ya rasimu asilia ya Kitabu Kitakatifu ambayo imehifadhiwa na Allah kwa namna fulani, kwa vipimo ambavyo havitambuliki kikamilifu na binadamu.

Aya 18. Hao watu wanampigia Allah mfano kuwa amechukua binti, kama wenyewe wapewe habari kuwa wamezaa watoto wa kike nyuso zao zinafifia kwa huzuni.

وَقَالُوْا لَوْ شَآءَ الرَّحْمٰنُ مَا عَبَدْنٰهُمْ ؕ مَا لَهُمْ بِذٰلِكَ مِنْ عِلْمٍ ۚ اِنْ هُمْ اِلَّا يَخْرُصُوْنَ ﴿٢١﴾

21. Na husema: Angalipenda Rahmani tusingewaabudu. Hawana elimu ya haya, hawasemi ila kukisia tu.

اَمْ اٰتَيْنٰهُمْ كِتٰبًا مِّنْ قَبْلِهٖ فَهُمْ بِهٖ مُسْتَمْسِكُوْنَ ﴿٢٢﴾

22. Je, Tumewapa Kitabu kabla ya hiki, nao wakakishika?

بَلْ قَالُوْٓا اِنَّا وَجَدْنَآ اٰبَآءَنَا عَلٰٓى اُمَّةٍ وَّاِنَّا عَلٰٓى اٰثٰرِهِمْ مُّهْتَدُوْنَ ﴿٢٣﴾

23. Bali wanasema: Hakika sisi tuliwakuta baba zetu juu ya desturi na bila shaka tutapata mwongozo kwa kufuata nyayo zao.

وَكَذٰلِكَ مَآ اَرْسَلْنَا مِنْ قَبْلِكَ فِيْ قَرْيَةٍ مِّنْ نَّذِيْرٍ اِلَّا قَالَ مُتْرَفُوْهَآ ۙ اِنَّا وَجَدْنَآ اٰبَآءَنَا عَلٰٓى اُمَّةٍ وَّاِنَّا عَلٰٓى اٰثٰرِهِمْ مُّقْتَدُوْنَ ﴿٢٤﴾

24. Na kadhalika Hatukumpeleka kabla yako, Mwonyaji katika mji wo wote ila matajiri wake walisema: Kwa yakini tuliwakuta baba zetu juu ya desturi na hakika sisi ni wenye kufuata tu nyayo zao.

قٰلَ اَوَلَوْ جِئْتُكُمْ بِاَهْدٰى مِمَّا وَجَدْتُّمْ عَلَيْهِ اٰبَآءَكُمْ ؕ قَالُوْٓا اِنَّا بِمَآ اُرْسِلْتُمْ بِهٖ كٰفِرُوْنَ ﴿٢٥﴾

25. Akasema: Hata kama nawaleteeni (desturi) yenye mwongozo bora kuliko mliyowakuta nayo baba zenu? Wakasema: Kwa hakika sisi tunayakataa yale mliyotumwa nayo.

فَانْتَقَمْنَا مِنْهُمْ فَانْظُرْ كَيْفَ كَانَ عَاقِبَةُ الْمُكَذِّبِيْنَ ﴿٢٦﴾ ع

26. Ndipo Tukawalipizia, basi angalia ulikuwaje mwisho wa wale waliokadhibisha.

FUNGU 3

وَاِذْ قَالَ اِبْرٰهِيْمُ لِاَبِيْهِ وَقَوْمِهٖٓ اِنَّنِيْ بَرَآءٌ مِّمَّا تَعْبُدُوْنَ ﴿٢٧﴾ ۙ

27. Na (kumbuka) Ibrahimu alipomwambia baba yake na watu wake: Bila shaka mimi ninajitenga mbali na hayo mnayoyaabudu.

اِلَّا الَّذِيْ فَطَرَنِيْ فَاِنَّهٗ سَيَهْدِيْنِ ﴿٢٨﴾

28. Isipokuwa Yeye Aliyeniumba; kwa yakini Yeye Ataniongoza.

وَجَعَلَهَا كَلِمَةًۢ بَاقِيَةً فِيْ عَقِبِهٖ لَعَلَّهُمْ يَرْجِعُوْنَ ﴿٢٩﴾

29. Na Akalifanya (neno) hili kuwa ishara kubwa yenye kubaki katika wazao wake ili warejee.

بَلْ مَتَّعْتُ هٰٓؤُلَآءِ وَاٰبَآءَهُمْ حَتّٰى جَآءَهُمُ الْحَقُّ وَرَسُوْلٌ مُّبِيْنٌ ﴿٣٠﴾

30. Bali Niliwafaidisha hawa na baba zao mpaka ikawafikia haki na Mtume abainishaye.

وَلَمَّا جَآءَهُمُ الْحَقُّ قَالُوْا هٰذَا سِحْرٌ وَّاِنَّا بِهٖ كٰفِرُوْنَ ﴿٣١﴾

31. Na ilipowafikia haki wakasema: Huu ni uchawi na hakika sisi ni wenye kuukataa.

وَقَالُوْا لَوْلَا نُزِّلَ هٰذَا الْقُرْاٰنُ عَلٰى رَجُلٍ مِّنَ الْقَرْيَتَيْنِ عَظِيْمٍ ﴿٣١﴾

32. Na wakasema: Mbona hii Kurani haikuteremshwa juu ya mtu mkubwa kutoka katika miji miwili maarufu?

اَهُمْ يَقْسِمُوْنَ رَحْمَتَ رَبِّكَ ؕ نَحْنُ قَسَمْنَا بَيْنَهُمْ مَّعِيْشَتَهُمْ فِى الْحَيٰوةِ الدُّنْيَا وَرَفَعْنَا بَعْضَهُمْ فَوْقَ بَعْضٍ دَرَجٰتٍ لِّيَتَّخِذَ بَعْضُهُمْ بَعْضًا سُخْرِيًّا ؕ وَرَحْمَتُ رَبِّكَ خَيْرٌ مِّمَّا يَجْمَعُوْنَ ﴿٣٢﴾

33. Je, ni wao wanaoigawa rehema ya Mola wako? Ni Sisi Tuliowagawanyia matumizi yao katika maisha ya dunia hii na Tumewainua baadhi yao daraja juu ya wengine, hivyo baadhi yao wanawafanya wengine kuwa watumishi; na rehema za Mola wako ni bora kuliko wanayoyakusanya.

وَلَوْلَآ اَنْ يَّكُوْنَ النَّاسُ اُمَّةً وَّاحِدَةً لَّجَعَلْنَا لِمَنْ يَّكْفُرُ بِالرَّحْمٰنِ لِبُيُوْتِهِمْ سُقُفًا مِّنْ فِضَّةٍ وَّ مَعَارِجَ عَلَيْهَا يَظْهَرُوْنَ ﴿٣٣﴾

34. Na isingekuwa watu watakuwa kundi moja, bila shaka Tungalifanya dari za nyumba za watu wanaomkufuru Rahmani, kwa fedha, na vivyo hivyo ngazi wanazozipanda,

وَلِبُيُوْتِهِمْ اَبْوَابًا وَّ سُرُرًا عَلَيْهَا يَتَّكِـُٔوْنَ ﴿٣٤﴾

35. Na milango ya nyumba zao na vitanda wanavyoviegemea,

وَزُخْرُفًا ؕ وَاِنْ كُلُّ ذٰلِكَ لَمَّا مَتَاعُ الْحَيٰوةِ الدُّنْيَا ؕ وَالْاٰخِرَةُ عِنْدَ رَبِّكَ لِلْمُتَّقِيْنَ ﴿٣٥﴾ ع ۳

36. Na dhahabu (pia); lakini hayo yote ni starehe tu ya maisha ya dunia, na Akhera mbele ya Mola wako ni kwa wamchao tu.

FUNGU 4

وَمَنْ يَّعْشُ عَنْ ذِكْرِ الرَّحْمٰنِ نُقَيِّضْ لَهٗ شَيْطٰنًا فَهُوَ لَهٗ قَرِيْنٌ ﴿٣٦﴾

37. Na anayegeuka asimkumbuke Rahmani Tunamwekea Shetani naye anakuwa rafiki yake.

Aya 32. *Miji miwili* ni Makka na Taif. Makafiri wanaweza kumfuata mtu mkubwa wa kidunia mwenye heshima na mali, lakini hawataki kumfuata mtu asiye na mali ambaye ametumwa na Allah.

Aya 33. *Je, wao wanaigawa rehema ya Mola wako?* Hapa makafiri wanajibiwa na Allah ya kuwa kazi ya kugawanya rehema Yake ni Yake Mwenyewe., naye ndiye anajua vizuri ni nani anayestahili kupewa jambo fulani. Basi si shauri ya makafiri kujiingiza katika kazi ya Allah, kwani kujiingiza kwao hakuna maana kwa vile Mungu amempa Mtume *s.a.w.* unabii kwa kujua ya kwamba yeye ndiye anayefaa.

Aya 37. Neno *Dhikr* katika Aya hii pia maana yake ni Kurani. Na mradi wa Aya ni kuwa mtu anayejigeuza mbali na Kurani, na kushika badala yake mafundisho mengine, basi yeye atapangwa urafiki na shetani

38. Na kwa yakini hao wanawazuilia njia nao hudhani ya kwamba hakika wao ndio wenye kuongoka.

وَاِنَّهُمْ لَيَصُدُّوْنَهُمْ عَنِ السَّبِيْلِ وَيَحْسَبُوْنَ اَنَّهُمْ مُّهْتَدُوْنَ ﴿٣٨﴾

39. Hata atakapotufikia atasema: Laiti ungalikuwako umbali wa mashariki na magharibi kati yangu na wewe, ni rafiki mbaya alioje!

حَتّٰٓى اِذَا جَآءَنَا قَالَ يٰلَيْتَ بَيْنِىْ وَبَيْنَكَ بُعْدَ الْمَشْرِقَيْنِ فَبِئْسَ الْقَرِيْنُ ﴿٣٩﴾

40. Na leo wakati ambapo mmeshadhulumu, kushirikiana kwenu katika adhabu hakutawafaeni kitu.

وَلَنْ يَّنْفَعَكُمُ الْيَوْمَ اِذْ ظَّلَمْتُمْ اَنَّكُمْ فِى الْعَذَابِ مُشْتَرِكُوْنَ ﴿٤٠﴾

41. Je, unaweza kumsikilizisha kiziwi, au unaweza kumwongoza kipofu na aliyomo katika upotevu ulio wazi?

اَفَاَنْتَ تُسْمِعُ الصُّمَّ اَوْ تَهْدِى الْعُمْىَ وَمَنْ كَانَ فِىْ ضَلٰلٍ مُّبِيْنٍ ﴿٤١﴾

42. Na kama Tukikuondoa, basi hakika Sisi Tutajilipiza kisasi kwao.

فَاِمَّا نَذْهَبَنَّ بِكَ فَاِنَّا مِنْهُمْ مُّنْتَقِمُوْنَ ﴿٤٢﴾

43. Au Tutakuonyesha Tuliyowaahidi Nasi bila shaka Tuna uwezo juu yao.

اَوْ نُرِيَنَّكَ الَّذِىْ وَعَدْنٰهُمْ فَاِنَّا عَلَيْهِمْ مُّقْتَدِرُوْنَ ﴿٤٣﴾

44. Basi yashike yaliyofunuliwa kwako; bila shaka umo katika njia iliyonyooka.

فَاسْتَمْسِكْ بِالَّذِىْٓ اُوْحِىَ اِلَيْكَ ۚ اِنَّكَ عَلٰى صِرَاطٍ مُّسْتَقِيْمٍ ﴿٤٤﴾

45. Na kwa yakini haya ni ukumbusho kwako na kwa watu wako na karibuni mtaulizwa.

وَاِنَّهٗ لَذِكْرٌ لَّكَ وَلِقَوْمِكَ ۚ وَسَوْفَ تُسْـَٔلُوْنَ ﴿٤٥﴾

46. Na kawaulize Mitume Wetu Tuliowapeleka kabla yako: je Tulifanya miungu mingine badala ya Rahmani iabudiwayo?

وَسْـَٔلْ مَنْ اَرْسَلْنَا مِنْ قَبْلِكَ مِنْ رُّسُلِنَآ اَجَعَلْنَا مِنْ دُوْنِ الرَّحْمٰنِ اٰلِهَةً يُّعْبَدُوْنَ ﴿٤٦﴾ ع

FUNGU 5

47. Na bila shaka Tulimtuma Musa na Aya Zetu kwa Firauni na wakuu wake, na akasema: Kwa yakini mimi ni Mjumbe wa Mola wa walimwengu.

وَلَقَدْ اَرْسَلْنَا مُوْسٰى بِاٰيٰتِنَآ اِلٰى فِرْعَوْنَ وَمَلَا۟ئِهٖ فَقَالَ اِنِّىْ رَسُوْلُ رَبِّ الْعٰلَمِيْنَ ﴿٤٧﴾

48. Lakini alipowafikia na Ishara Zetu, mara wao wakazicheka!

فَلَمَّا جَآءَهُمْ بِاٰيٰتِنَآ اِذَا هُمْ مِّنْهَا يَضْحَكُوْنَ ﴿٤٨﴾

وَمَا نُرِيْهِمْ مِّنْ اٰيَةٍ اِلَّا هِيَ اَكْبَرُ مِنْ اُخْتِهَا ۖ وَاَخَذْنٰهُمْ بِالْعَذَابِ لَعَلَّهُمْ يَرْجِعُوْنَ ﴿٤٩﴾

49. Na Hatukuwaonyesha Ishara yo yote ila hiyo ilikuwa kubwa zaidi kuliko yenziwe. Na Tukawakamata kwa adhabu ili warejee.

وَقَالُوْا يٰٓاَيُّهَ السّٰحِرُ ادْعُ لَنَا رَبَّكَ بِمَا عَهِدَ عِنْدَكَ ۚ اِنَّنَا لَمُهْتَدُوْنَ ﴿٥٠﴾

50. Na wakasema: Ewe mchawi! Utuombee kwa Mola wako kwa yale Aliyokuahidi, kwa yakini tutakuwa wenye kuongoka.

فَلَمَّا كَشَفْنَا عَنْهُمُ الْعَذَابَ اِذَا هُمْ يَنْكُثُوْنَ ﴿٥١﴾

51. Basi Tulipowaondolea adhabu, mara wakavunja (mapatano).

وَنَادٰى فِرْعَوْنُ فِيْ قَوْمِهٖ قَالَ يٰقَوْمِ اَلَيْسَ لِيْ مُلْكُ مِصْرَ وَهٰذِهِ الْاَنْهٰرُ تَجْرِيْ مِنْ تَحْتِيْ ۚ اَفَلَا تُبْصِرُوْنَ ﴿٥٢﴾

52. Na Firauni alitangaza katika watu wake, akasema: Enyi watu wangu! je, utawala wa Misri si wangu, na pia mito hii ipitayo chini ya himaya yangu? Je, hamwoni?

اَمْ اَنَا خَيْرٌ مِّنْ هٰذَا الَّذِيْ هُوَ مَهِيْنٌ ۙ وَّلَا يَكَادُ يُبِيْنُ ﴿٥٣﴾

53. Au mimi si bora kuliko huyu asiye na hadhi yoyote, wala hawezi kusema waziwazi.

فَلَوْلَآ اُلْقِيَ عَلَيْهِ اَسْوِرَةٌ مِّنْ ذَهَبٍ اَوْ جَآءَ مَعَهُ الْمَلٰٓئِكَةُ مُقْتَرِنِيْنَ ﴿٥٤﴾

54. Basi mbona hakuteremshiwa bangili za dhahabu, au kuja pamoja naye makundi ya malaika?

فَاسْتَخَفَّ قَوْمَهٗ فَاَطَاعُوْهُ ۭ اِنَّهُمْ كَانُوْا قَوْمًا فٰسِقِيْنَ ﴿٥٥﴾

55. Na akawahafifisha watu wake, nao wakaanza kumtii; kwa hakika wao walikuwa watu waasi.

فَلَمَّآ اٰسَفُوْنَا انْتَقَمْنَا مِنْهُمْ فَاَغْرَقْنٰهُمْ اَجْمَعِيْنَ ﴿٥٦﴾

56. Basi walipotukasirisha, Tukawalipiza kisasi na Tukawagharikisha wote.

فَجَعَلْنٰهُمْ سَلَفًا وَّمَثَلًا لِّلْاٰخِرِيْنَ ﴿٥٧﴾ ع

57. Kisha Tukawafanya kuwa hadithi za kale na onyo kwa watu wa baadaye.

FUNGU 6

وَلَمَّا ضُرِبَ ابْنُ مَرْيَمَ مَثَلًا اِذَا قَوْمُكَ مِنْهُ يَصِدُّوْنَ ﴿٥٨﴾

58. Na anapotajwa mwana wa Mariamu kwa namna ya mfano ndipo watu wako wanaupigia kelele.

وَقَالُوْٓا ءَاٰلِهَتُنَا خَيْرٌ اَمْ هُوَ ۭ مَا ضَرَبُوْهُ لَكَ اِلَّا جَدَلًا ۭ بَلْ هُمْ قَوْمٌ خَصِمُوْنَ ﴿٥٩﴾

59. Na husema: Je, miungu yetu ni bora au yeye? Hawakuelezi hayo ila kwa kujadiliana tu; bali hao ni watu wagombanao.

60. Yeye siye ila ni mtumishi Tuliyemneemesha na Tukamfanya methali kwa wana wa Israeli.

إِنْ هُوَ إِلَّا عَبْدٌ أَنْعَمْنَا عَلَيْهِ وَجَعَلْنٰهُ مَثَلًا لِّبَنِيٓ إِسْرَآءِيلَ ﴿٥٩﴾

61. Na kama Tungalipenda Tungewafanya Malaika miongoni mwenu kuwa makhalifa katika ardhi·

وَلَوْ نَشَآءُ لَجَعَلْنَا مِنكُم مَّلٰٓئِكَةً فِى الْأَرْضِ يَخْلُفُونَ ﴿٦٠﴾

62. Lakini kwa yakini yeye ni elimu ya Saa ile. Kwa hiyo msiifanyie shaka na mnifuate. Hii ndiyo njia iliyo sahihi.

وَإِنَّهُۥ لَعِلْمٌ لِّلسَّاعَةِ فَلَا تَمْتَرُنَّ بِهَا وَاتَّبِعُونِ ۚ هٰذَا صِرَاطٌ مُّسْتَقِيمٌ ﴿٦١﴾

63. Wala asiwazuieni Shetani: bila shaka kwenu yeye ni adui dhahiri.

وَلَا يَصُدَّنَّكُمُ الشَّيْطٰنُ ۚ إِنَّهُۥ لَكُمْ عَدُوٌّ مُّبِينٌ ﴿٦٢﴾

64. Na alipofika Isa kwa dalili zilizo wazi, akasema: Nimewajieni na hekima na ili niwaelezeni baadhi ya yale mnayohitilafiana, basi mcheni Allah na mnitii.

وَلَمَّا جَآءَ عِيسٰى بِالْبَيِّنٰتِ قَالَ قَدْ جِئْتُكُم بِالْحِكْمَةِ وَلِأُبَيِّنَ لَكُم بَعْضَ الَّذِى تَخْتَلِفُونَ فِيهِ ۖ فَاتَّقُوا اللَّهَ وَأَطِيعُونِ ﴿٦٣﴾

65. Kwa hakika Allah ndiye Mola wangu na Mola wenu, basi Mwabuduni; hii ndiyo njia iliyonyooka.

إِنَّ اللَّهَ هُوَ رَبِّى وَرَبُّكُمْ فَاعْبُدُوهُ ۚ هٰذَا صِرَاطٌ مُّسْتَقِيمٌ ﴿٦٤﴾

66. Lakini makundi yakahitilafiana wao kwa wao, basi ole kwa wale waliodhulumu kwa adhabu ya siku iumizayo.

فَاخْتَلَفَ الْأَحْزَابُ مِنۢ بَيْنِهِمْ ۖ فَوَيْلٌ لِّلَّذِينَ ظَلَمُوا مِنْ عَذَابِ يَوْمٍ أَلِيمٍ ﴿٦٥﴾

67. Hawangojei ila saa iwafikie kwa ghafla hali hawatambui.

هَلْ يَنظُرُونَ إِلَّا السَّاعَةَ أَن تَأْتِيَهُم بَغْتَةً وَهُمْ لَا يَشْعُرُونَ ﴿٦٦﴾

68. Marafiki wakubwa siku hiyo watakuwa maadui wao kwa wao, ila wamchao (Allah)

ٱلْأَخِلَّآءُ يَوْمَئِذٍۭ بَعْضُهُمْ لِبَعْضٍ عَدُوٌّ إِلَّا الْمُتَّقِينَ ﴿٦٧﴾ ع ١٢

Aya 62. Neno *saa'atu* ambalo tafsiri yake ya neno kwa neno ni 'saa' ni lazima lieleweke kwa maana ile ile kama lilivyotumika katika Suuratul Qamar aya ya 2 (54:2). Pale, mabadiliko ya kimapinduzi ambayo yalikuwa lazima yatokee wakati wa ujio wa Mtukufu Mtume Muhammad s.a.w. yanaelezwa kuwa ni *saa'atu*. Na kupasuka kwa mwezi kumeletwa kama ushahidi wa kuunga mkono mapinduzi ya kiroho ambayo yalikuwa yanakaribia kutokea. Maana ya neno hili kama linavyotumika kumhusu Yesu kwenye aya inayochunguzwa ni lazima ieleweke kwa misingi ile ile. Hivyo basi 'saa' ina maana ya ujio wa Yesu katika siku za baadae na yale mapinduzi ya kiroho yatakayoambatana na saa hiyo.

FUNGU 7

69. Enyi watumishi Wangu! Leo hakutakuwa na hofu yoyote juu yenu wala hamtahuzunika.

يٰعِبَادِ لَا خَوْفٌ عَلَيْكُمُ الْيَوْمَ وَلَآ اَنْتُمْ تَحْزَنُوْنَ ۚ﴿٦٩﴾

70. Wale walioziamini Ishara Zetu na wakawa wenye kutii.

اَلَّذِيْنَ اٰمَنُوْا بِاٰيٰتِنَا وَكَانُوْا مُسْلِمِيْنَ ۚ﴿٧٠﴾

71. Ingieni katika Bustani, ninyi na wake zenu katika hali ya kufurahishwa mno.

اُدْخُلُوا الْجَنَّةَ اَنْتُمْ وَاَزْوَاجُكُمْ تُحْبَرُوْنَ ﴿٧١﴾

72. Watatembezewa sahani za dhahabu na vikombe, na humo vitakuwamo ambavyo nafsi zinavipenda na macho yatavifurahia, na ninyi mtakaa humo.

يُطَافُ عَلَيْهِمْ بِصِحَافٍ مِّنْ ذَهَبٍ وَّاَكْوَابٍ ۚ وَفِيْهَا مَا تَشْتَهِيْهِ الْاَنْفُسُ وَتَلَذُّ الْاَعْيُنُ ۚ وَاَنْتُمْ فِيْهَا خٰلِدُوْنَ ۚ﴿٧٢﴾

73. Na hii ni Bustani mliyorithishwa kwa hayo mliyokuwa mkiyafanya.

وَتِلْكَ الْجَنَّةُ الَّتِيْٓ اُوْرِثْتُمُوْهَا بِمَا كُنْتُمْ تَعْمَلُوْنَ ﴿٧٣﴾

74. Yamo humo matunda mengi kwa ajili yenu mtakayoyala

لَكُمْ فِيْهَا فَاكِهَةٌ كَثِيْرَةٌ مِّنْهَا تَاْكُلُوْنَ ﴿٧٤﴾

75. Kwa hakika wakosefu ni wenye kukaa muda mrefu ndani ya adhabu ya Jahannamu.

اِنَّ الْمُجْرِمِيْنَ فِيْ عَذَابِ جَهَنَّمَ خٰلِدُوْنَ ۖ﴿٧٥﴾

76. Hawatapunguziwa na humo watakata tamaa.

لَا يُفَتَّرُ عَنْهُمْ وَهُمْ فِيْهِ مُبْلِسُوْنَ ۚ﴿٧٦﴾

77. Wala Sisi Hatukuwadhulumu bali wao wenyewe walikuwa wadhalimu.

وَمَا ظَلَمْنٰهُمْ وَلٰكِنْ كَانُوْا هُمُ الظّٰلِمِيْنَ ﴿٧٧﴾

78. Nao wataita; Ewe mlinzi wa Jahannamu, na atufishe Mola wako. Atajibu: Ninyi ni wenye kubakia humu humu.

وَنَادَوْا يٰمٰلِكُ لِيَقْضِ عَلَيْنَا رَبُّكَ ؕ قَالَ اِنَّكُمْ مّٰكِثُوْنَ ﴿٧٨﴾

79. Kwa yakini Tumewaleteeni haki, lakini wengi wenu ni waichukiao haki.

لَقَدْ جِئْنٰكُمْ بِالْحَقِّ وَلٰكِنَّ اَكْثَرَكُمْ لِلْحَقِّ كٰرِهُوْنَ ﴿٧٩﴾

80. Au wamekata shauri la kufanya lolote? basi Sisi pia tumeshakata shauri la kufanya chochote.

اَمْ اَبْرَمُوْٓا اَمْرًا فَاِنَّا مُبْرِمُوْنَ ۚ﴿٨٠﴾

81. Au wanawaza ya kwamba Hatuzisikii siri zao na mashauriano yao ya siri? Naam! na Wajumbe Wetu huwa karibu nao wakiyaandika.

اَمْ يَحْسَبُوْنَ اَنَّا لَا نَسْمَعُ سِرَّهُمْ وَنَجْوٰىهُمْ ؕ بَلٰى وَرُسُلُنَا لَدَيْهِمْ يَكْتُبُوْنَ ﴿٨١﴾

82. Sema: Kama Rahmani Angalikuwa na mwana ningekuwa wa kwanza wa wanaoabudu.

قُلْ اِنْ كَانَ لِلرَّحْمٰنِ وَلَدٌ ۖ فَاَنَا اَوَّلُ الْعٰبِدِيْنَ ﴿٨١﴾

83. Ameepukana - Mola wa mbingu na ardhi, Mola wa Arshi - na hayo wanayomsifia.

سُبْحٰنَ رَبِّ السَّمٰوٰتِ وَالْاَرْضِ رَبِّ الْعَرْشِ عَمَّا يَصِفُوْنَ ﴿٨٢﴾

84. Basi waache wapige porojo na wacheze mpaka wakutane na Siku yao wanayoahidiwa.

فَذَرْهُمْ يَخُوْضُوْا وَيَلْعَبُوْا حَتّٰى يُلٰقُوْا يَوْمَهُمُ الَّذِىْ يُوْعَدُوْنَ ﴿٨٣﴾

85. Na Yeye ndiye Anayeabudiwa mbinguni na Anayeabudiwa ardhini; naye ni Mwenye hekima, Mwenye elimu.

وَهُوَ الَّذِىْ فِى السَّمَآءِ اِلٰهٌ وَّفِى الْاَرْضِ اِلٰهٌ ؕ وَهُوَ الْحَكِيْمُ الْعَلِيْمُ ﴿٨٤﴾

86. Na Mwenye mibaraka ni Yule Ambaye ufalme wa mbingu na ardhi na vilivyomo kati yao ni Wake, na iko Kwake elimu ya saa ile na Kwake mtarudishwa.

وَتَبٰرَكَ الَّذِىْ لَهٗ مُلْكُ السَّمٰوٰتِ وَالْاَرْضِ وَمَا بَيْنَهُمَا ۚ وَعِنْدَهٗ عِلْمُ السَّاعَةِ ۚ وَاِلَيْهِ تُرْجَعُوْنَ ﴿٨٥﴾

87. Wala hawana uwezo wa uombezi wale wanaowaomba badala Yake, ila anayeishuhudia haki, nao wanajua.

وَلَا يَمْلِكُ الَّذِيْنَ يَدْعُوْنَ مِنْ دُوْنِهِ الشَّفَاعَةَ اِلَّا مَنْ شَهِدَ بِالْحَقِّ وَهُمْ يَعْلَمُوْنَ ﴿٨٦﴾

88. Na ukiwauliza ni nani Aliyewaumba? Kwa yakini watasema: Allah; basi ni wapi wanakogeuzwa?

وَلَئِنْ سَاَلْتَهُمْ مَّنْ خَلَقَهُمْ لَيَقُوْلُنَّ اللّٰهُ فَاَنّٰى يُؤْفَكُوْنَ ﴿٨٧﴾

89. Na usemi wake (wa kila) mara ni: Ee Mola wangu, kwa yakini hawa ni watu wasioamini.

وَقِيْلِهٖ يٰرَبِّ اِنَّ هٰٓؤُلَآءِ قَوْمٌ لَّا يُؤْمِنُوْنَ ﴿٨٨﴾ ۘ

90. Basi waache na useme: Amani. Hivi karibuni watajua.

فَاصْفَحْ عَنْهُمْ وَقُلْ سَلٰمٌ ؕ فَسَوْفَ يَعْلَمُوْنَ ﴿٨٩﴾ ع ۲۲ ۱۳

سُوْرَةُ الدُّخَانِ مَكِّيَّةٌ وَّ هِيَ مَعَ الْبَسْمَلَةِ سِتُّوْنَ اٰيَةً وَّ ثَلَاثَةُ رُكُوْعَاتٍ

44. SURA AD-DUKHAAN

Imeteremshwa Makka

Ina mafungu 3 na Aya 60 pamoj ana Bismillahi

1. Kwa jina la Allah, Mwingi wa rehema, Mwingi wa ukarimu.

بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ ١

2. Ahimidiwaye, Atukuzwaye.

حٰمٓ ۚ ٢

3. Naapa kwa Kitabu kinachobainisha;

وَالْكِتٰبِ الْمُبِيْنِ ۙ ٣

معانقة ١٢ عند المتقدمين

4. Kwa yakini Tumeiteremsha (Kurani) katika usiku uliobarikiwa - bila shaka Sisi Tulikuwa ni Waonyao.

اِنَّآ اَنْزَلْنٰهُ فِيْ لَيْلَةٍ مُّبٰرَكَةٍ اِنَّا كُنَّا مُنْذِرِيْنَ ٤

5. Katika (usiku) huu huamuliwa kila suala la hekima.

فِيْهَا يُفْرَقُ كُلُّ اَمْرٍ حَكِيْمٍ ۙ ٥

6. Ndiyo hukumu iliyotoka Kwetu; kwa hakika Sisi ni Watumao.

اَمْرًا مِّنْ عِنْدِنَا ؕ اِنَّا كُنَّا مُرْسِلِيْنَ ۚ ٦

7. Ni rehema itokayo kwa Mola wako; bila shaka Yeye ndiye Asikiaye, Ajuaye.

رَحْمَةً مِّنْ رَّبِّكَ ؕ اِنَّهٗ هُوَ السَّمِيْعُ الْعَلِيْمُ ۙ ٧

8. Mola wa mbingu na ardhi na vilivyomo kati yao, ikiwa mnayo yakini.

رَبِّ السَّمٰوٰتِ وَالْاَرْضِ وَمَا بَيْنَهُمَا ۘ اِنْ كُنْتُمْ مُّوْقِنِيْنَ ٨

وقف لازم

9. Hakuna Aabudiwaye ila Yeye, Anahuisha na kufisha, ni Mola wenu na pia Mola wa baba zenu wa mwanzo.

لَآ اِلٰهَ اِلَّا هُوَ يُحْيٖ وَيُمِيْتُ ؕ رَبُّكُمْ وَرَبُّ اٰبَآئِكُمُ الْاَوَّلِيْنَ ٩

10. Lakini hao wamo katika shaka wakicheza.

بَلْ هُمْ فِيْ شَكٍّ يَّلْعَبُوْنَ ١٠

Sura hii ilishuka Makka, na imepewa jina toka Aya ya 11.

Aya 2. *Haa Miim* (Tazama sura zilizopita).

Aya 4. *Usiku uliobarikiwa* walivyokubaliana mufasirina ni usiku wa *Lailatul Qadr* ulioelezwa katika sura 97:2, ambao unatokea katika siku 10 za mwisho wa mwezi wa Ramadhani. Kadhalika watu wanapokuwa katika upotevu wanahesabiwa kuwa wamo katika usiku wa giza. Wakati inapofika nuru ya Mjumbe ye yote wa Allah, siku ile inaitwa, *Usiku uliobarikiwa.*

فَارْتَقِبْ يَوْمَ تَاْتِي السَّمَآءُ بِدُخَانٍ مُّبِيْنٍ ﴿١١﴾

11. Basi ungoje siku ambayo mbingu itakapoleta moshi dhahiri.

يَّغْشَى النَّاسَ ؕ هٰذَا عَذَابٌ اَلِيْمٌ ﴿١٢﴾

12. Utakaowafunika watu; hii ni adhabu iumizayo.

رَبَّنَا اكْشِفْ عَنَّا الْعَذَابَ اِنَّا مُؤْمِنُوْنَ ﴿١٣﴾

13. Mola wetu, tuondolee adhabu hii; hakika tutaamini.

اَنّٰى لَهُمُ الذِّكْرٰى وَ قَدْ جَآءَهُمْ رَسُوْلٌ مُّبِيْنٌ ﴿١٤﴾

14. Wataupataje ukumbusho? Na amekwisha wafikia Mtume abainishaye,

ثُمَّ تَوَلَّوْا عَنْهُ وَقَالُوْا مُعَلَّمٌ مَّجْنُوْنٌ ﴿١٥﴾

15. Kisha wakampa kisogo na wakasema: Amefunzwa, (bali) ni mwendawazimu.

اِنَّا كَاشِفُوا الْعَذَابِ قَلِيْلًا اِنَّكُمْ عَآئِدُوْنَ ﴿١٦﴾

16. Kwa yakini Sisi Tutaiondoa adhabu (kwa muda) kidogo, (lakini) ninyi mtayarudia mambo hayo hayo.

يَوْمَ نَبْطِشُ الْبَطْشَةَ الْكُبْرٰى ۚ اِنَّا مُنْتَقِمُوْنَ ﴿١٧﴾

17. S iku Tutakayokamata mkamato mkubwa: Hakika sisi ni wenye kulipiza kisasi.

وَلَقَدْ فَتَنَّا قَبْلَهُمْ قَوْمَ فِرْعَوْنَ وَجَآءَهُمْ رَسُوْلٌ كَرِيْمٌ ﴿١٨﴾

18. Na hakika kabla ya hawa Tuliwajaribu watu wa Firauni na aliwafikia Mtume aheshimiwaye.

اَنْ اَدُّوْۤا اِلَيَّ عِبَادَ اللّٰهِ ؕ اِنِّيْ لَكُمْ رَسُوْلٌ اَمِيْنٌ ﴿١٩﴾

19. (Akisema,) nirudishieni watumishi wa Allah, kwa hakika mimi ni Mtume mwaminifu Kwenu;

وَّاَنْ لَّا تَعْلُوْا عَلَى اللّٰهِ ۚ اِنِّيْۤ اٰتِيْكُمْ بِسُلْطٰنٍ مُّبِيْنٍ ﴿٢٠﴾

20. Na msimuasi Allah, mimi kwa yakini ni mwenye kuwaleteeni dalili iliyo wazi.

وَ اِنِّيْ عُذْتُ بِرَبِّيْ وَ رَبِّكُمْ اَنْ تَرْجُمُوْنِ ﴿٢١﴾

21. Nami najikinga kwa Mola wangu na Mola wenu ili msinipige mawe.

وَاِنْ لَّمْ تُؤْمِنُوْا لِيْ فَاعْتَزِلُوْنِ ﴿٢٢﴾

22. Na kama hamniamini basi jitengeni nami.

Aya 11. *Dukhaan,* "Moshi." Neno hili pia lina maana ya *Jadab*, yaani upungufu au ukame na njaa (Taj). Njaa imeitwa "moshi" kwa sababu ya ukame wa nchi ambao vumbi lake hufanana na moshi. Mradi wake ni njaa ile iliyotokea kwa Makureishi kwa miaka saba.

Imam Bukhari anasimulia ya kwamba Makureishi walipozidi kumpinga Mtume *s.a.w.*, aliomba waadhibiwe kwa njaa kama iliyotokea siku za Nabii Yusuf. Basi Makureishi walipata njaa kali kwa miaka saba hata wakawa wanakula mifupa na mizoga, nao walipokuwa wakitazama mbinguni walikuwa wanaona kama moshi kwa ajili ya shida.

Kadhalika inasimuliwa ya kwamba kabla ya Kiyama utatokea moshi.

فَدَعَا رَبَّهٗۤ اَنَّ هٰۤؤُلَآءِ قَوْمٌ مُّجْرِمُوْنَ ﴿٢٣﴾

23. Ndipo akamwomba Mola wake kwamba hawa ni watu wahalifu.

فَاَسْرِ بِعِبَادِیْ لَیْلًا اِنَّكُمْ مُّتَّبَعُوْنَ ﴿٢٤﴾

24. Basi nenda pamoja na watumishi Wangu usiku, hakika ninyi ni wenye kufuatwa.

وَ اتْرُكِ الْبَحْرَ رَهْوًا ؕ اِنَّهُمْ جُنْدٌ مُّغْرَقُوْنَ ﴿٢٥﴾

25. Na uiache bahari inapokupwa; hakika wao ni jeshi litakalozamishwa.

كَمْ تَرَكُوْا مِنْ جَنّٰتٍ وَّ عُیُوْنٍ ﴿٢٦﴾

26. Mabustani mangapi na chemchem waliziacha!

وَّ زُرُوْعٍ وَّ مَقَامٍ كَرِیْمٍ ﴿٢٧﴾

27. Na mashamba na makamu ya heshima na taadhima!

وَّ نَعْمَةٍ كَانُوْا فِیْهَا فٰكِهِیْنَ ﴿٢٨﴾

28. Na neema walizokuwamo wakijifurahisha;

كَذٰلِكَ ۫ وَ اَوْرَثْنٰهَا قَوْمًا اٰخَرِیْنَ ﴿٢٩﴾

29. Ndivyo ilivyokuwa, na Tukazirithisha watu wengine.

فَمَا بَكَتْ عَلَیْهِمُ السَّمَآءُ وَ الْاَرْضُ وَ مَا كَانُوْا مُنْظَرِیْنَ ﴿٣٠﴾

30. Mbingu na ardhi havikuwalilia, wala hawakupewa muhula.

FUNGU 2

وَ لَقَدْ نَجَّیْنَا بَنِیْۤ اِسْرَآءِیْلَ مِنَ الْعَذَابِ الْمُهِیْنِ ﴿٣١﴾

31. Na bila shaka Tuliwaokoa wana wa Israeli katika adhabu ifedheheshayo,

مِنْ فِرْعَوْنَ ؕ اِنَّهٗ كَانَ عَالِیًا مِّنَ الْمُسْرِفِیْنَ ﴿٣٢﴾

32. Ya Firauni; hakika yeye alikuwa jeuri katika wapitao kiasi.

وَ لَقَدِ اخْتَرْنٰهُمْ عَلٰی عِلْمٍ عَلَی الْعٰلَمِیْنَ ﴿٣٣﴾

33. Na Tukawachagua kwa elimu kuliko walimwengu (wengine).

وَ اٰتَیْنٰهُمْ مِّنَ الْاٰیٰتِ مَا فِیْهِ بَلٰٓؤٌا مُّبِیْنٌ ﴿٣٤﴾

34. Na Tukawapa Ishara zilizokuwa na majaribio yaliyo wazi.

اِنَّ هٰۤؤُلَآءِ لَیَقُوْلُوْنَ ﴿٣٥﴾

35. Hakika hao wanasema:

اِنْ هِیَ اِلَّا مَوْتَتُنَا الْاُوْلٰی وَ مَا نَحْنُ بِمُنْشَرِیْنَ ﴿٣٦﴾

36. Hayo siyo ila ni mauti yetu ya kwanza wala sisi hatutafufuliwa.

Aya 25. *Rawh*, "Inapokupwa." Neno hili lina maana ya "kutulia," "nafasi iliyo baina ya vitu viwili," "upana wa njia" (Taj na Mufradat).

Jambo hasa lililotokea ni hili. Waisraeli walipofika kando ya bahari kimbunga kikaanza kuvuma na maji yakapwa, njia ikapatikana, nao wakapita (sura 26:64-67). Firauni alipofika akakuta maji yamekupwa kama desturi na akafikiri kuwa atawahi kupita mpaka ng'ambo na kumshika Musa. Alipofika ndani ya bahari maji yakarudii na kumgharikisha pamoja na majeshi yake. Habari hii imeelezwa mahali pengine katika sura hizi zifuatazo: 2:51; 7:137; 8:55; 20:78, 81; 28:41.

فَأْتُوْا بِاٰبَآئِنَآ اِنْ كُنْتُمْ صٰدِقِيْنَ ﴿٣٦﴾

37. Basi warudisheni baba zetu, ikiwa mnasema kweli!

اَهُمْ خَيْرٌ اَمْ قَوْمُ تُبَّعٍ ۙ وَّالَّذِيْنَ مِنْ قَبْلِهِمْ ؕ اَهْلَكْنٰهُمْ ۫ اِنَّهُمْ كَانُوْا مُجْرِمِيْنَ ﴿٣٧﴾

38. Je, wao ni bora au watu wa Tubba na wale waliokuwa kabla yao? Tuliwaangamiza, kwa yakini wao walikuwa wakosefu.

وَمَا خَلَقْنَا السَّمٰوٰتِ وَالْاَرْضَ وَمَا بَيْنَهُمَا لٰعِبِيْنَ ﴿٣٨﴾

39. Na Hatukuziumba mbingu na ardhi na vilivyomo kati yao kwa mchezo.

مَا خَلَقْنٰهُمَآ اِلَّا بِالْحَقِّ وَلٰكِنَّ اَكْثَرَهُمْ لَا يَعْلَمُوْنَ ﴿٣٩﴾

40. Hatukuviumba ila kwa haki, lakini wengi wao hawajui.

اِنَّ يَوْمَ الْفَصْلِ مِيْقَاتُهُمْ اَجْمَعِيْنَ ﴿٤٠﴾ ۙ

41. Kwa yakini siku ya hukumu ni wakati uliowekwa kwa wao wote.

يَوْمَ لَا يُغْنِيْ مَوْلًى عَنْ مَّوْلًى شَيْـًٔا وَّلَا هُمْ يُنْصَرُوْنَ ﴿٤١﴾ ۙ

42. Siku ambayo rafiki hatamfaa rafiki cho chote, wala hawatanusuriwa.

اِلَّا مَنْ رَّحِمَ اللّٰهُ ؕ اِنَّهٗ هُوَ الْعَزِيْزُ الرَّحِيْمُ ﴿٤٢﴾ ع

43. Ila yule Allah Atakayemrehemu; hakika Yeye ndiye Mwenye ushindi kamili, Mrehemevu.

FUNGU 3

اِنَّ شَجَرَتَ الزَّقُّوْمِ ﴿٤٣﴾ ۙ

44. Bila shaka mti wa Zakkum,

طَعَامُ الْاَثِيْمِ ﴿٤٤﴾ ۖ

45. Ni chakula cha mwenye dhambi.

كَالْمُهْلِ ۚ يَغْلِيْ فِي الْبُطُوْنِ ﴿٤٥﴾ ۙ

46. Kama shaba iliyoyeyuka; huchemka matumboni-

كَغَلْيِ الْحَمِيْمِ ﴿٤٦﴾

47. Kama mchemko wa maji ya moto.

خُذُوْهُ فَاعْتِلُوْهُ اِلٰى سَوَآءِ الْجَحِيْمِ ﴿٤٧﴾ ۖ

48. Mkamateni na mburureni mpaka katikati ya Jahanamu.

ثُمَّ صُبُّوْا فَوْقَ رَاْسِهٖ مِنْ عَذَابِ الْحَمِيْمِ ﴿٤٨﴾ ؕ

49. Kisha mmwagieni adhabu ya maji ya moto kichwani mwake.

ذُقْ ۚ اِنَّكَ اَنْتَ الْعَزِيْزُ الْكَرِيْمُ ﴿٤٩﴾

50. Onja! Hakika wewe (ulijifanya) mwenye nguvu, mheshimiwa!

Aya 38. *Watu wa Tubba.* Tubba ni jina la lakabu la wafalme wa Bani Himya waliokuwa wanatawala Yaman (Kashshaf Jami'ul Bayan).

Aya 50. Tazama sura 37:63.

51. Hakika hii ndiyo mliyokuwa mkibishana.

اِنَّ هٰذَا مَا كُنْتُمْ بِهٖ تَمْتَرُوْنَ ﴿٥١﴾

52. Bila shaka wale wamchao Allah watakuwa katika mahali pa amani.

اِنَّ الْمُتَّقِيْنَ فِيْ مَقَامٍ اَمِيْنٍ ﴿٥٢﴾

53. Katika Mabustani na chemchem.

فِيْ جَنّٰتٍ وَّعُيُوْنٍ ﴿٥٣﴾

54. Watavaa hariri laini na hariri nzito; wakielekeana.

يَّلْبَسُوْنَ مِنْ سُنْدُسٍ وَّ اِسْتَبْرَقٍ مُّتَقٰبِلِيْنَ ﴿٥٤﴾

55. Hivi ndivyo itakavyokuwa; na Tutawaoza mahuurin-aini (wanawake warembo wenye macho makubwa).

كَذٰلِكَ ۗ وَزَوَّجْنٰهُمْ بِحُوْرٍ عِيْنٍ ﴿٥٥﴾

56. Humo wataomba kila aina ya matunda, wakikaa kwa amani

يَدْعُوْنَ فِيْهَا بِكُلِّ فَاكِهَةٍ اٰمِنِيْنَ ﴿٥٦﴾

57. Humo hawataonja mauti ila mauti yale ya kwanza na Atawalinda na adhabu ya Jahanamu.

لَا يَذُوْقُوْنَ فِيْهَا الْمَوْتَ اِلَّا الْمَوْتَةَ الْاُوْلٰى ۚ وَوَقٰىهُمْ عَذَابَ الْجَحِيْمِ ﴿٥٧﴾

58. Kwa fadhili zitokazo kwa Mola wako huu ndiyo ufaulu mkuu.

فَضْلًا مِّنْ رَّبِّكَ ۭ ذٰلِكَ هُوَ الْفَوْزُ الْعَظِيْمُ ﴿٥٨﴾

59. Basi Tumeifanya nyepesi kwa ulimi wako ili washike nasaha.

فَاِنَّمَا يَسَّرْنٰهُ بِلِسَانِكَ لَعَلَّهُمْ يَتَذَكَّرُوْنَ ﴿٥٩﴾

60. Kwa hiyo ngoja, hakika wao (pia) wanangoja.

فَارْتَقِبْ اِنَّهُمْ مُّرْتَقِبُوْنَ ﴿٦٠﴾ ع ٣ ١٦

سُوْرَةُ الْجَاثِيَةِ مَكِّيَّةٌ وَّ هِيَ مَعَ الْبَسْمَلَةِ ثَمَانٍ وَّ ثَلَا ثُوْنَ اٰيَةً وَّ اَرْبَعَةُ رُكُوْعَاتٍ

45. SURA AL-JAATHIYA

Imeteremshwa Makka

Ina mafungu 4 na Aya 38 pamoja na Bismillahi

بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ ①

1. Kwa jina la Allah, Mwingi wa rehema, Mwingi wa ukarimu.

حٰمٓ ②

2. Ahimidiwaye, Atukuzwaye.

تَنْزِيْلُ الْكِتٰبِ مِنَ اللّٰهِ الْعَزِيْزِ الْحَكِيْمِ ③

3. Uteremsho wa Kitabu umetoka kwa Allah, Mwenye ushindi kamili, Mwenye hekima.

اِنَّ فِي السَّمٰوٰتِ وَالْاَرْضِ لَاٰيٰتٍ لِّلْمُؤْمِنِيْنَ ④

4. Bila shaka katika mbingu na ardhi zimo Ishara kwa ajili ya waaminio

وَفِيْ خَلْقِكُمْ وَمَا يَبُثُّ مِنْ دَآبَّةٍ اٰيٰتٌ لِّقَوْمٍ يُّوْقِنُوْنَ ⑤

5. Na katika kuumbwa kwenu na katika wanyama Aliowatawanya zimo Ishara kwa watu wenye yakini.

وَاخْتِلَافِ الَّيْلِ وَالنَّهَارِ وَمَآ اَنْزَلَ اللّٰهُ مِنَ السَّمَآءِ مِنْ رِّزْقٍ فَاَحْيَا بِهِ الْاَرْضَ بَعْدَ مَوْتِهَا وَتَصْرِيْفِ الرِّيٰحِ اٰيٰتٌ لِّقَوْمٍ يَّعْقِلُوْنَ ⑥

6. Na (katika) kupishana usiku na mchana na (katika) riziki Aliyoteremsha Allah kutoka mawinguni na Akaifufua kwayo ardhi baada ya kufa kwake na mabadiliko ya pepo, zimo Ishara kwa watu wenye akili.

تِلْكَ اٰيٰتُ اللّٰهِ نَتْلُوْهَا عَلَيْكَ بِالْحَقِّ ۚ فَبِاَيِّ حَدِيْثٍ بَعْدَ اللّٰهِ وَاٰيٰتِهٖ يُؤْمِنُوْنَ ⑦

7. Hizo ndizo Ishara za Allah Tunazokusomea kwa haki; basi hadithi gani watakayoamini baada ya Allah na Aya Zake?

Sura hii ilishuka Makka, na imepewa jina toka Aya 29.

Aya 2. *Haa Miim* (Tazama sura zilizopita).

Aya 7. *Hadithi gani watakayoamini.* Hapa imeelezwa ya kuwa Hadithi zinazotakiwa kuaminiwa ni zile zisizokwenda kinyume na maneno ya Kurani. Ni wazi ya kuwa watu wengi walitunga hadithi za uwongo wakasema ziimesimuliwa na Mtume s.a.w. Hivyo hadithi na iwe katika Kitabu gani itakubaliwa kwa sharti hii tu ya kuwa haipinzani na maagizo na maneno ya Kurani.

8. Maangamizo kwa kila atungaye uwongo, mwenye dhambi.

وَيْلٌ لِّكُلِّ اَفَّاكٍ اَثِيْمٍ ۙ﴿٨﴾

9. Anasikia Aya za Allah zikisomwa juu yake kisha hushikilia kujivuna kana kwamba hakuzisikia; basi umpe habari ya adhabu iumizayo.

يَّسْمَعُ اٰيٰتِ اللّٰهِ تُتْلٰى عَلَيْهِ ثُمَّ يُصِرُّ مُسْتَكْبِرًا كَاَنْ لَّمْ يَسْمَعْهَا ۚ فَبَشِّرْهُ بِعَذَابٍ اَلِيْمٍ ﴿٩﴾

10. Na anapojua kidogo katika Aya Zetu huzifanyia mzaha. Watu hao ndio watakuwa na adhabu ifedheheshayo.

وَاِذَا عَلِمَ مِنْ اٰيٰتِنَا شَيْـًٔا اتَّخَذَهَا هُزُوًا ؕ اُولٰٓئِكَ لَهُمْ عَذَابٌ مُّهِيْنٌ ﴿١٠﴾

11. Na nyuma yao iko Jahanamu, wala waliyoyachuma hayatawafaa hata kidogo, wala walinzi waliowashika badala ya Allah; na watapata adhabu kubwa.

مِنْ وَّرَآئِهِمْ جَهَنَّمُ ۚ وَلَا يُغْنِىْ عَنْهُمْ مَّا كَسَبُوْا شَيْـًٔا وَّلَا مَا اتَّخَذُوْا مِنْ دُوْنِ اللّٰهِ اَوْلِيَآءَ ۚ وَلَهُمْ عَذَابٌ عَظِيْمٌ ﴿١١﴾

12. Huu ni mwongozo mkubwa; lakini wale waliozikataa Aya za Mola wao watakuwa na adhabu yenye maumivu iumizayo.

هٰذَا هُدًى ۚ وَالَّذِيْنَ كَفَرُوْا بِاٰيٰتِ رَبِّهِمْ لَهُمْ عَذَابٌ مِّنْ رِّجْزٍ اَلِيْمٌ ﴿١٢﴾

FUNGU 2

13. Allah Ndiye Aliyewatiishieni bahari ili humo zipite merikebu kwa amri Yake, na ili mtafute fadhili Yake na mpate kushukuru.

اَللّٰهُ الَّذِىْ سَخَّرَ لَكُمُ الْبَحْرَ لِتَجْرِىَ الْفُلْكُ فِيْهِ بِاَمْرِهٖ وَلِتَبْتَغُوْا مِنْ فَضْلِهٖ وَلَعَلَّكُمْ تَشْكُرُوْنَ ﴿١٣﴾

14. Na Amewatiishieni vilivyomo mbinguni na vilivyomo ardhini - vyote vimetoka Kwake; bila shaka katika hayo zimo Ishara kwa watu wanaotafakari.

وَسَخَّرَ لَكُمْ مَّا فِى السَّمٰوٰتِ وَمَا فِى الْاَرْضِ جَمِيْعًا مِّنْهُ ؕ اِنَّ فِىْ ذٰلِكَ لَاٰيٰتٍ لِّقَوْمٍ يَّتَفَكَّرُوْنَ ﴿١٤﴾

Aya 8. *Wail,* " Maangamizo." Inasemekana ya kuwa *wail* ni bonde moja katika Jahanamu. Hapa wanaomkadhibisha Mtume *s.a.w.* wanaambiwa ya kuwa mwisho wao utakuwa maangamizo na kutupwa ndani ya *Jahanamu.*

Aya 13-14. Mwanadamu anatakiwa kufikiri ya kuwa vitu vyote vimetiishwa kwa ajili yake, basi je naye ameumbwa kwa kusudi gani? Hakuna kusudi jingine aliloumbiwa isipokuwa kumwabudu Allah na kumjua na kuchukua sifa Zake kwa kuwasaidia viumbe Wake wengine.

15. Waambie wale walioamini wawasamehe wale ambao hawatazamii kwamba siku zilizoahidiwa za Allah zitakuja kutokea, ili Awalipe watu kwa yale wanayoyachuma.

قُلْ لِّلَّذِيْنَ اٰمَنُوْا يَغْفِرُوْا لِلَّذِيْنَ لَا يَرْجُوْنَ اَيَّامَ اللّٰهِ لِيَجْزِيَ قَوْمًا بِمَا كَانُوْا يَكْسِبُوْنَ ﴿١٥﴾

16. Mwenye kutenda wema basi ni kwa ajili ya nafsi yake, na mwenye kufanya uovu ni juu yake; kisha mtarudishwa kwa Mola wenu.

مَنْ عَمِلَ صَالِحًا فَلِنَفْسِهٖ ۚ وَمَنْ اَسَآءَ فَعَلَيْهَا ۗ ثُمَّ اِلٰى رَبِّكُمْ تُرْجَعُوْنَ ﴿١٦﴾

17. Na kwa yakini Tuliwapa wana wa Israeli Kitabu na hukumu, na unabii na Tukawapa vitu vizuri na Tukawafadhili kuliko walimwengu.

وَلَقَدْ اٰتَيْنَا بَنِيْٓ اِسْرَآءِيْلَ الْكِتٰبَ وَالْحُكْمَ وَالنُّبُوَّةَ وَرَزَقْنٰهُمْ مِّنَ الطَّيِّبٰتِ وَفَضَّلْنٰهُمْ عَلَى الْعٰلَمِيْنَ ﴿١٧﴾ ۚ

18. Na Tukawapa maelezo ya amri, basi hawakuhitilafiana ila baada ya kuwafikia elimu, kwa uasi baina yao; hakika Mola wako Atahukumu kati yao siku ya Kiyama katika yale waliyokuwa wakihitilafiana.

وَاٰتَيْنٰهُمْ بَيِّنٰتٍ مِّنَ الْاَمْرِ ۚ فَمَا اخْتَلَفُوْٓا اِلَّا مِنْۢ بَعْدِ مَا جَآءَهُمُ الْعِلْمُ ۙ بَغْيًۢا بَيْنَهُمْ ۭ اِنَّ رَبَّكَ يَقْضِيْ بَيْنَهُمْ يَوْمَ الْقِيٰمَةِ فِيْمَا كَانُوْا فِيْهِ يَخْتَلِفُوْنَ ﴿١٨﴾

19. Kisha Tumekuweka juu ya sheria hasa katika amri, basi ifuate, wala usifuate matamanio ya wale wasiojua.

ثُمَّ جَعَلْنٰكَ عَلٰى شَرِيْعَةٍ مِّنَ الْاَمْرِ فَاتَّبِعْهَا وَلَا تَتَّبِعْ اَهْوَآءَ الَّذِيْنَ لَا يَعْلَمُوْنَ ﴿١٩﴾

20. Kwa yakini hao hawatakufaa cho chote mbele ya Allah; na hakika wadhalimu ni marafiki wao kwa wao, na Allah ni rafiki wa wamchao.

اِنَّهُمْ لَنْ يُّغْنُوْا عَنْكَ مِنَ اللّٰهِ شَيْـًٔا ۭ وَاِنَّ الظّٰلِمِيْنَ بَعْضُهُمْ اَوْلِيَآءُ بَعْضٍ ۚ وَاللّٰهُ وَلِيُّ الْمُتَّقِيْنَ ﴿٢٠﴾

21. Hizi ni dalili zilizo wazi kwa watu, nazo ni mwongozo na rehema kwa watu wenye yakini.

هٰذَا بَصَآئِرُ لِلنَّاسِ وَهُدًى وَّرَحْمَةٌ لِّقَوْمٍ يُّوْقِنُوْنَ ﴿٢١﴾

22. Je! Wanafikiri wale waliofanya maovu kuwa Tutawafanya kama wale walioamini na kutenda mema - kwamba maisha yao na mauti yao yawe sawa? Ni mabaya wanayoyahukumu.

اَمْ حَسِبَ الَّذِيْنَ اجْتَرَحُوا السَّيِّاٰتِ اَنْ نَّجْعَلَهُمْ كَالَّذِيْنَ اٰمَنُوْا وَعَمِلُوا الصّٰلِحٰتِ ۙ سَوَآءً مَّحْيَاهُمْ وَمَمَاتُهُمْ ۭ سَآءَ مَا يَحْكُمُوْنَ ﴿٢٢﴾ ع

Aya 15. *Siku za Allah,* ni siku zile ambazo watu wanapewa mafanikio au wanaangamizwa.

FUNGU 3

23. Na Allah Ameziumba mbingu na ardhi kwa haki na ili kila nafsi ilipwe yale iliyoyachuma; nao hawatadhulumiwa.

وَخَلَقَ اللّٰهُ السَّمٰوٰتِ وَالْاَرْضَ بِالْحَقِّ وَلِتُجْزٰى كُلُّ نَفْسٍۢ بِمَا كَسَبَتْ وَهُمْ لَا يُظْلَمُوْنَ ﴿٢٣﴾

24. Je, umemwona yule aliyefanya tamaa yake kuwa Mola wake, na ambaye Allah Alimhukumu kupotea kwa msingi wa elimu fulani, na akapiga muhuri juu ya masikio yake na moyo wake, na Akaweka pazia machoni mwake? Basi ni nani atakyemuongoza baada ya Allah? Basi je hata hivyo hamtashika nasaha?

اَفَرَءَيْتَ مَنِ اتَّخَذَ اِلٰهَهٗ هَوٰىهُ وَاَضَلَّهُ اللّٰهُ عَلٰى عِلْمٍ وَّخَتَمَ عَلٰى سَمْعِهٖ وَقَلْبِهٖ وَجَعَلَ عَلٰى بَصَرِهٖ غِشٰوَةً ؕ فَمَنْ يَّهْدِيْهِ مِنْۢ بَعْدِ اللّٰهِ ؕ اَفَلَا تَذَكَّرُوْنَ ﴿٢٣﴾

25. Nao husema: Haya siyo ila ni maisha tu ya dunia; tunakufa na tunaishi wala hakuna kinachotuangamiza isipokuwa dahari (zama). Lakini wao hawana elimu ya hayo ila wanadhani tu.

وَقَالُوْا مَا هِىَ اِلَّا حَيَاتُنَا الدُّنْيَا نَمُوْتُ وَنَحْيَا وَمَا يُهْلِكُنَآ اِلَّا الدَّهْرُ ۚ وَمَا لَهُمْ بِذٰلِكَ مِنْ عِلْمٍ ۚ اِنْ هُمْ اِلَّا يَظُنُّوْنَ ﴿٢٤﴾

26. Na wanaposomewa Aya Zetu zilizo wazi hawana hoja ila kusema: Waleteni baba zetu ikiwa ninyi ni wasemao kweli.

وَاِذَا تُتْلٰى عَلَيْهِمْ اٰيٰتُنَا بَيِّنٰتٍ مَّا كَانَ حُجَّتَهُمْ اِلَّآ اَنْ قَالُوا ائْتُوْا بِاٰبَآئِنَآ اِنْ كُنْتُمْ صٰدِقِيْنَ ﴿٢٥﴾

27. Sema: Allah Huwapeni uzima kisha Huwafisheni, kisha Atawakusanyeni siku ya Kiyama - haina shaka; lakini watu wengi hawajui.

قُلِ اللّٰهُ يُحْيِيْكُمْ ثُمَّ يُمِيْتُكُمْ ثُمَّ يَجْمَعُكُمْ اِلٰى يَوْمِ الْقِيٰمَةِ لَا رَيْبَ فِيْهِ وَلٰكِنَّ اَكْثَرَ النَّاسِ لَا يَعْلَمُوْنَ ﴿٢٦﴾ ع ١٩

FUNGU 4

28. Na ufalme wa mbingu na ardhi ni wa Allah; na siku itakapotokea saa ile, siku hiyo wasemao uongo watapata hasara.

وَلِلّٰهِ مُلْكُ السَّمٰوٰتِ وَالْاَرْضِ ؕ وَيَوْمَ تَقُوْمُ السَّاعَةُ يَوْمَئِذٍ يَّخْسَرُ الْمُبْطِلُوْنَ ﴿٢٧﴾

29. Na utawaona kila taifa wakipiga magoti, kila taifa litaitwa kwenye kitabu

وَتَرٰى كُلَّ اُمَّةٍ جَاثِيَةً ۛ كُلُّ اُمَّةٍ تُدْعٰٓى اِلٰى كِتٰبِهَا ؕ اَلْيَوْمَ تُجْزَوْنَ مَا كُنْتُمْ

Aya 29. *Wakipiga magoti,* yaani watakuwa katika msiba mkubwa. Aya hii inaonyesha ya

chake; leo mtalipwa yale mliyokuwa mkiyatenda.

تَعْمَلُوْنَ ﴿٢٩﴾

30. Hiki ni kitabu Chetu kitakachobainisha dhidi yenu kwa haki bila shaka Tulikuwa Tukiyaandika yale mliyokuwa mkiyatenda.

هٰذَا كِتٰبُنَا يَنْطِقُ عَلَيْكُمْ بِالْحَقِّ ۚ اِنَّا كُنَّا نَسْتَنْسِخُ مَا كُنْتُمْ تَعْمَلُوْنَ ﴿٣٠﴾

31. Lakini wale walioamini na wakatenda mema, Mola wao Atawaingiza katika rehema Yake; hayo ndiyo mafanikio ya wazi wazi.

فَاَمَّا الَّذِيْنَ اٰمَنُوْا وَعَمِلُوا الصّٰلِحٰتِ فَيُدْخِلُهُمْ رَبُّهُمْ فِيْ رَحْمَتِهٖ ۚ ذٰلِكَ هُوَ الْفَوْزُ الْمُبِيْنُ ﴿٣١﴾

32. Waama wale waliokufuru (watatambiwa): Je, hazikuwa Aya Zangu zikisomwa kwenu; nanyi mkajivuna na mmekuwa watu wahalifu?

وَاَمَّا الَّذِيْنَ كَفَرُوْا ۗ اَفَلَمْ تَكُنْ اٰيٰتِيْ تُتْلٰى عَلَيْكُمْ فَاسْتَكْبَرْتُمْ وَكُنْتُمْ قَوْمًا مُّجْرِمِيْنَ ﴿٣٢﴾

33. Na iliposemwa: hakika ahadi ya Allah ni kweli, na saa ile haina shaka, mkasema: Hatujui saa ile ni nini; hatudhani ila kukisia tu wala sisi si wenye yakini.

وَاِذَا قِيْلَ اِنَّ وَعْدَ اللّٰهِ حَقٌّ وَّالسَّاعَةُ لَا رَيْبَ فِيْهَا قُلْتُمْ مَّا نَدْرِيْ مَا السَّاعَةُ ۙ اِنْ نَّظُنُّ اِلَّا ظَنًّا وَّمَا نَحْنُ بِمُسْتَيْقِنِيْنَ ﴿٣٣﴾

34. Na ubaya wa waliyoyatenda utawadhirikia na yatawazunguka yale waliyoyafanyia mzaha.

وَبَدَا لَهُمْ سَيِّاٰتُ مَا عَمِلُوْا وَحَاقَ بِهِمْ مَّا كَانُوْا بِهٖ يَسْتَهْزِءُوْنَ ﴿٣٤﴾

35. Na itasemwa: Leo Tunawasahauni kama ninyi mlivyosahau mkutano wa siku yenu hii, na mahali penu ni Motoni, wala hamna wasaidizi.

وَقِيْلَ الْيَوْمَ نَنْسٰىكُمْ كَمَا نَسِيْتُمْ لِقَآءَ يَوْمِكُمْ هٰذَا وَمَاْوٰىكُمُ النَّارُ وَمَا لَكُمْ مِّنْ نّٰصِرِيْنَ ﴿٣٥﴾

---

kuwa mataifa pia yatahukumiwa mbele ya Allah kwa matendo yao kama vile yanavyohukumiwa hapa duniani.

Litaitwa kwenye kitabu chake. Yaani watahukumiwa sawa na Sheria ya Kitabu walichopewa, au watahukumiwa sawa na dafatari ya vitendo vyao.

Aya 32. *Fastakbartum*, "Mkajivuna." *Istikbar* maana yake ni kuwa mtu si mkubwa lakini anapenda ajulikane kuwa yu mkubwa.

Aya 35. *Tunawasahauni.* Siyo matlabu yake kuwa Mungu anasahau, bali mradi wake ni "Tunawaacheni" kana kwamba mliosahauliwa.

ذٰلِكُمْ بِاَنَّكُمُ اتَّخَذْتُمْ اٰيٰتِ اللّٰهِ هُزُوًا وَّ غَرَّتْكُمُ الْحَيٰوةُ الدُّنْيَا ۚ فَالْيَوْمَ لَا يُخْرَجُوْنَ مِنْهَا وَلَا هُمْ يُسْتَعْتَبُوْنَ ﴿٣٥﴾

36. Hayo ni kwa sababu mlizifanyia mzaha Ishara za Allah, na maisha ya dunia yakawadanganyeni. Basi leo hawatatolewa humo, wala hautakubaliwa udhuru wao wowote.

فَلِلّٰهِ الْحَمْدُ رَبِّ السَّمٰوٰتِ وَ رَبِّ الْاَرْضِ رَبِّ الْعٰلَمِيْنَ ﴿٣٦﴾

37. Basi sifa zote njema ni za Allah, Mola wa mbingu na Mola wa ardhi, Mola wa walimwengu.

وَلَهُ الْكِبْرِيَآءُ فِى السَّمٰوٰتِ وَ الْاَرْضِ ۚ وَهُوَ الْعَزِيْزُ الْحَكِيْمُ ﴿٣٧﴾

38. Na ukubwa ni Wake mbinguni na ardhini naye ni Mwenye ushindi kamili, Mwenye hekima.

Aya 37. Itakapotokea saa ile inayotajwa katika Aya 33 itajulikana kuwa Allah ndiye Mwenye kila sifa njema, na aliye Mwumba wa mbingu na ardhi na Mwumba wa walimwengu wote. Mambo yatakayotokea saa ile yatahakikisha ya kuwa Ukubwa hasa ni wa Allah katika mbingu na ardhi, naye ni bila shaka Mwenye hekima.

سُوْرَةُ الْاَحْقَافِ مَكِّيَّةٌ وَّ هِيَ مَعَ الْبَسْمَلَةِ سِتٌّ وَّ ثَلَاثُوْنَ اٰيَةً وَّاَرْبَعَةُ رُكُوْعَاتٍ

46. SURA AL-AHQAAF

Imeteremshwa Makka

Ina mafungu 4 na Aya 36 pamoja na Bismillahi

JUZU 26

بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ ①

1. Kwa jina la Allah, Mwingi wa rehema, Mwingi wa ukarimu.

حٰمٓ ②

2. Ahimidiwaye, Atukuzwaye.

تَنْزِيْلُ الْكِتٰبِ مِنَ اللّٰهِ الْعَزِيْزِ الْحَكِيْمِ ③

3. Uteremsho wa Kitabu hiki umetoka kwa Allah, Mwenye ushindi kamili, Mwenye hekima.

مَا خَلَقْنَا السَّمٰوٰتِ وَالْاَرْضَ وَمَا بَيْنَهُمَآ اِلَّا بِالْحَقِّ وَاَجَلٍ مُّسَمًّى ؕ وَالَّذِيْنَ كَفَرُوْا عَمَّآ اُنْذِرُوْا مُعْرِضُوْنَ ④

4. Hatukuziumba mbingu na ardhi na vilivyomo kati yao ila kwa haki na kwa muda uliowekwa; na wale wanaokufuru huyapuuza wanayoonywa.

قُلْ اَرَءَيْتُمْ مَّا تَدْعُوْنَ مِنْ دُوْنِ اللّٰهِ اَرُوْنِيْ مَاذَا خَلَقُوْا مِنَ الْاَرْضِ اَمْ لَهُمْ شِرْكٌ فِي السَّمٰوٰتِ ؕ اِيْتُوْنِيْ بِكِتٰبٍ مِّنْ قَبْلِ هٰذَآ اَوْ اَثٰرَةٍ مِّنْ عِلْمٍ اِنْ كُنْتُمْ صٰدِقِيْنَ ⑤

5. Sema: Je, mmewaona mnaowaita kinyume cha Allah? Nionyesheni kipi walichokiumba katika ardhi, au wanao ushirika katika mbingu? Nileteeni Kitabu kilichokuwa kabla ya hiki au alama yo yote ya elimu ikiwa mnasema kweli.

Hii ndiyo sura ya mwisho katika fungu la *Haa Miim* na imepewa jina toka Aya 22, nayo sura hii ilishuka Makka.

Aya 2. *Haa Miim* ni maneno ya mkato kwa ajili ya sifa mbili za Allah. *Haa* ni *Hamiid* (Ahimidiwaye au asifiwaye); *Miim* ni *Majiid* (Atukuzwaye).

Aya 4. *Kwa haki,* maneno haya yanaonyesha ya kuwa ilikuwapo haja ya kwamba vitu hivi viumbwe kwa ajili ya kumfaa mwanadamu, havikuumbwa bila kuhitajiwa, bali ilikuwapo haja ya haki ya kwamba viwepo.

Muda uliowekwa. Maneno haya yamewekwa kuwakumbusha wale wanaozama katika mambo ya dunia na kumsahau Allah ya kuwa mambo ya dunia hii yana muda maalumu tu na kuna siku yatapita, hivyo wasipoteze bure wakati wao, bali waangalie mambo ya Akhera ambayo yatadumu milele.

Aya 5. *Nionyesheni kipi walichokiumba.* Hao wanaosadiki ya kuwa Nabii Isa alipata

6. Na ni nani mpotevu mkubwa kuliko yule anayemwomba asiyekuwa Allah ambaye hatamjibu mpaka siku ya Kiyama, nao hata hawazitambui dua zao.

وَمَنْ اَضَلُّ مِمَّنْ يَّدْعُوْا مِنْ دُوْنِ اللّٰهِ مَنْ لَّا يَسْتَجِيْبُ لَهٗۤ اِلٰى يَوْمِ الْقِيٰمَةِ وَهُمْ عَنْ دُعَآىِٕهِمْ غٰفِلُوْنَ ۝٦

7. Na watu watakapokusanywa, (wale walioombwa) watakuwa maadui zao, nao wataikataa ibada yao.

وَاِذَا حُشِرَ النَّاسُ كَانُوْا لَهُمْ اَعْدَآءً وَّكَانُوْا بِعِبَادَتِهِمْ كٰفِرِيْنَ ۝٧

8. Na wanaposomewa Aya Zetu zilizo wazi, wale waliokufuru husema juu ya haki inapowajia: Huu ni uchawi dhahiri.

وَاِذَا تُتْلٰى عَلَيْهِمْ اٰيٰتُنَا بَيِّنٰتٍ قَالَ الَّذِيْنَ كَفَرُوْا لِلْحَقِّ لَمَّا جَآءَهُمْ ۙ هٰذَا سِحْرٌ مُّبِيْنٌ ۝٨

9. Au husema: Ameyatunga mwenyewe. Sema: Ikiwa nimeyatunga mimi, basi hamwezi kunifaa cho chote mbele ya Allah; Yeye ndiye Ajuaye sana mnayoyashughulikia. Yeye Ametosha kuwa Shahidi kati yangu na yenu, naye ni Msamehevu, Mrehemevu.

اَمْ يَقُوْلُوْنَ افْتَرٰىهُ ؕ قُلْ اِنِ افْتَرَيْتُهٗ فَلَا تَمْلِكُوْنَ لِيْ مِنَ اللّٰهِ شَيْـًٔا ؕ هُوَ اَعْلَمُ بِمَا تُفِيْضُوْنَ فِيْهِ ؕ كَفٰى بِهٖ شَهِيْدًۢا بَيْنِيْ وَبَيْنَكُمْ ؕ وَهُوَ الْغَفُوْرُ الرَّحِيْمُ ۝٩

10. Sema: Mimi si mpya katika Mitume, wala sijui nitakavyofanywa mimi wala mtakavyofanywa ninyi. Sifuati ila yanayofunuliwa kwangu; na mimi siye ila ni Mwonyaji dhahiri.

قُلْ مَا كُنْتُ بِدْعًا مِّنَ الرُّسُلِ وَمَاۤ اَدْرِيْ مَا يُفْعَلُ بِيْ وَلَا بِكُمْ ؕ اِنْ اَتَّبِعُ اِلَّا مَا يُوْحٰۤى اِلَيَّ وَمَاۤ اَنَا اِلَّا نَذِيْرٌ مُّبِيْنٌ ۝١٠

---

kuumba vitu sasa watokee kujibu hoja hii ya Allah, na waonyeshe viko wapi alivyoumba. Sifa ya kuumba ni ya Allah tu, hakushirikiana na ye yote. Miungu ya uwongo ingekuwa miungu bila shaka tungeona vitu ilivyoviumba

Nileteeni Kitabu. Maneno haya yanaonyesha ya kuwa katika mambo ya itikadi na imani lazima ufuatwe ufunuo wa Kitabu cha Allah. Ndiyo maana imesemwa washirikina waonyeshe katika kitabu cha Mungu habari za itikadi zao. Mambo ya itikadi hayafuatwi kwa kusikiasikia maneno au rai za watu, bali yawe maagizo ya Allah Mwenyewe.

Aya 8. *Huu ni uchawi dhahiri.* Haya ndiyo maneno ya watu wanaokufuru. Wanaposhindwa katika dalili na uwazi wa Ishara za Mungu, wanakimbilia kusema kuwa yote hayo yasingeweza kufanyika ila kwa sababu ya uchawi.

Aya 10. *Mimi si mpya katika Mitume.* Hapa Mtume *s.a.w.* anawaambia watu ya kuwa yeye si Mtume mpya au wa kwanza kufika duniani, bali Mitume wengi walimtangulia na ambao watu wanawaamini, basi pia watazame je hakufanana na Mitume hao? Hii ndiyo alama mojawapo ya kuwatambua Manabii wakweli wanapofika. Kama atufikie Mtume ye yote tutazame je, amefanana na Mitume waliopita zamani?

قُلْ اَرَءَيْتُمْ اِنْ كَانَ مِنْ عِنْدِ اللّٰهِ
وَكَفَرْتُمْ بِهٖ وَشَهِدَ شَاهِدٌ مِّنْ
بَنِيْٓ اِسْرَآءِيْلَ عَلٰى مِثْلِهٖ فَاٰمَنَ
وَاسْتَكْبَرْتُمْ ؕ اِنَّ اللّٰهَ لَا يَهْدِى
الْقَوْمَ الظّٰلِمِيْنَ ﴿١١﴾ ع

11. Sema: Mwaonaje ikiwa kama imetoka kwa Allah nanyi mmeikataa, na shahidi miongoni mwa wana wa Israeli alishuhudia juu ya mfano wake na akaamini, lakini ninyi mnafanya kiburi; kwa yakini Allah Hawaongozi watu wadhalimu.

FUNGU 2

وَقَالَ الَّذِيْنَ كَفَرُوْا لِلَّذِيْنَ اٰمَنُوْا لَوْ كَانَ
خَيْرًا مَّا سَبَقُوْنَآ اِلَيْهِ ؕ وَاِذْ لَمْ يَهْتَدُوْا بِهٖ
فَسَيَقُوْلُوْنَ هٰذَآ اِفْكٌ قَدِيْمٌ ﴿١٢﴾

12. Na waliokufuru wakawaambia waaminio: Kama hilo lingekuwa jambo jema msingetutangulia kwalo. Na wanapokosa kuongoka kwayo, basi husema: huu ni uwongo wa zamani.

وَمِنْ قَبْلِهٖ كِتٰبُ مُوْسٰٓى اِمَامًا وَّرَحْمَةً ؕ
وَهٰذَا كِتٰبٌ مُّصَدِّقٌ لِّسَانًا عَرَبِيًّا لِّيُنْذِرَ
الَّذِيْنَ ظَلَمُوْا ۖ وَبُشْرٰى لِلْمُحْسِنِيْنَ ﴿١٣﴾ ۚ

13. Na kabla yake kilikuwapo Kitabu cha Musa kiongozi na chenye rehema. Na hiki ni Kitabu chenye kusadikisha, cha lugha ya Kiarabu, ili kiwaonye wale waliodhulumu na chenye habari za furaha kwa watendao wema.

اِنَّ الَّذِيْنَ قَالُوْا رَبُّنَا اللّٰهُ ثُمَّ اسْتَقَامُوْا
فَلَا خَوْفٌ عَلَيْهِمْ وَلَا هُمْ يَحْزَنُوْنَ ﴿١٤﴾ ۚ

14. Hakika wale waliosema, Mola wetu ni Allah, kisha wakadumu imara, haitakuwa hofu juu yao wala hawatahuzunika.

اُولٰٓئِكَ اَصْحٰبُ الْجَنَّةِ خٰلِدِيْنَ فِيْهَا ۚ
جَزَآءًۢ بِمَا كَانُوْا يَعْمَلُوْنَ ﴿١٥﴾

15. Hao ndio watu wa Peponi, watakaa humo: ni malipo ya yale waliyokuwa wakiyatenda.

Aya 13. *Chenye kusadikisha.* Mahali pengi Kurani imesemwa inasadikisha Vitabu vya zamani, yaani inaonyesha habari zilizo kweli katika Vitabu vile na zilizo uwongo. Na ndivyo ilivyofanya Kurani. Imebainisha makosa mengi yaliyoingia katika Vitabu vya zamani na kuonyesha habari zao zilizo sahihi.

Aya 14. Mahali penigne imesemwa hivi: *Hakika wale wanaosema, Mola wetu ni Allah, kisha wakaendelea kwa kudumu, huwateremkia Malaika (wakiwaambia): Msiogope wala msihuzunike, na furahieni Pepo mliyokuwa mkiahidiwa* (sura 41:31). Aya hizi zinaonyesha ya kwamba ingawa waaminio hutaabishwa hapa duniani na kutiwa mashakani, lakini Allah huwafariji kwa kuwateremshia Malaika wanaowapa habari njema ambazo zinawatoa huzuni na hofu na wanakuwa imara katika imani. Habari hizi hupata ama kwa ufunuo au *ilham* au njozi na ndoto.

16. Na Tumemwusia mwanadamu afanye wema kwa wazazi wake; mama yake ameibeba mimba yake kwa taabu na akamzaa kwa taabu; na mimba yake na (hadi) kumwachisha ziwa ni miezi thelathini; hata anapofikia balehe yake na akawa mwenye umri wa miaka arobaini, akasema: Ee Mola wangu, Uniwezeshe nizishukuru neema Zako ulizonineemesha mimi na wazazi wangu, na ili nifanye vitendo vizuri Unavyovipenda, na Unirekebishie pia na vizazi vyangu; kwa yakini ninatubu Kwako; na hakika mimi ni miongoni mwa waliosilimu.

وَوَصَّيْنَا الْاِنْسَانَ بِوَالِدَيْهِ اِحْسٰنًا ؕ حَمَلَتْهُ اُمُّهٗ كُرْهًا وَّوَضَعَتْهُ كُرْهًا ؕ وَحَمْلُهٗ وَفِصٰلُهٗ ثَلٰثُوْنَ شَهْرًا ؕ حَتّٰۤى اِذَا بَلَغَ اَشُدَّهٗ وَبَلَغَ اَرْبَعِيْنَ سَنَةً ۙ قَالَ رَبِّ اَوْزِعْنِيْۤ اَنْ اَشْكُرَ نِعْمَتَكَ الَّتِيْۤ اَنْعَمْتَ عَلَيَّ وَعَلٰى وَالِدَيَّ وَاَنْ اَعْمَلَ صَالِحًا تَرْضٰىهُ وَاَصْلِحْ لِيْ فِيْ ذُرِّيَّتِيْ ۚ اِنِّيْ تُبْتُ اِلَيْكَ وَاِنِّيْ مِنَ الْمُسْلِمِيْنَ ﴿١٦﴾

17. Hao ndio Tunaowakubali vitendo vyao vyema walivyovifanya, na Tunayapita kando makosa yao, watakuwa miongoni mwa watu wa Peponi: ahadi ya kweli waliyoahidiwa.

اُولٰٓئِكَ الَّذِيْنَ نَتَقَبَّلُ عَنْهُمْ اَحْسَنَ مَا عَمِلُوْا وَنَتَجَاوَزُ عَنْ سَيِّاٰتِهِمْ فِيْۤ اَصْحٰبِ الْجَنَّةِ ؕ وَعْدَ الصِّدْقِ الَّذِيْ كَانُوْا يُوْعَدُوْنَ ﴿١٧﴾

18. Na ambaye awaambiaye wazazi wake: Kefule ninyi! Je, mnaniogofisha ya kuwa nitatolewa na hali vizazi vingi vilikwisha pita kabla yangu? Na hao wawili huomba msaada wa Allah; (nao humwambia mtoto wao): Ole wako! Amini, hakika ahadi ya Allah ni ya kweli. Basi yeye husema: Hivi sivyo ila ni visa vya watu wa kale.

وَالَّذِيْ قَالَ لِوَالِدَيْهِ اُفٍّ لَّكُمَاۤ اَتَعِدٰنِنِيْۤ اَنْ اُخْرَجَ وَقَدْ خَلَتِ الْقُرُوْنُ مِنْ قَبْلِيْ ۚ وَهُمَا يَسْتَغِيْثٰنِ اللّٰهَ وَيْلَكَ اٰمِنْ ۖ اِنَّ وَعْدَ اللّٰهِ حَقٌّ ۚ فَيَقُوْلُ مَا هٰذَاۤ اِلَّاۤ اَسَاطِيْرُ الْاَوَّلِيْنَ ﴿١٨﴾

19. Hao ndio ambao imehakiki kauli juu yao, pamoja na mataifa yaliyopita kabla yao ya majinni na watu, hakika hao ndio waliokuwa wamepata hasara.

اُولٰٓئِكَ الَّذِيْنَ حَقَّ عَلَيْهِمُ الْقَوْلُ فِيْۤ اُمَمٍ قَدْ خَلَتْ مِنْ قَبْلِهِمْ مِّنَ الْجِنِّ وَالْاِنْسِ ؕ اِنَّهُمْ كَانُوْا خٰسِرِيْنَ ﴿١٩﴾

20. Na wote wana madaraja kwa yale waliyoyatenda, na ili (Mungu) Awalipe malipo ya vitendo vyao, nao hawatadhulumiwa.

وَلِكُلٍّ دَرَجٰتٌ مِّمَّا عَمِلُوْا ۚ وَلِيُوَفِّيَهُمْ اَعْمَالَهُمْ وَهُمْ لَا يُظْلَمُوْنَ ﴿٢٠﴾

وَيَوْمَ يُعْرَضُ الَّذِيْنَ كَفَرُوْا عَلَى النَّارِ ؕ
اَذْهَبْتُمْ طَيِّبٰتِكُمْ فِيْ حَيَاتِكُمُ الدُّنْيَا
وَاسْتَمْتَعْتُمْ بِهَا ۚ فَالْيَوْمَ تُجْزَوْنَ عَذَابَ
الْهُوْنِ بِمَا كُنْتُمْ تَسْتَكْبِرُوْنَ فِي
الْاَرْضِ بِغَيْرِ الْحَقِّ وَبِمَا كُنْتُمْ
تَفْسُقُوْنَ ﴿٢٠﴾ ع

21. Na siku watakapowekwa waliokufuru mbele ya Moto: Mlipoteza vitu vyenu vyote vizuri katika maisha yenu ya dunia, nanyi mlijinufaisha navyo, basi leo mtapewa adhabu ya fedheha kwa sababu mlijivuna bure duniani, na kwa sababu mlikuwa mkiasi.

FUNGU 3

وَاذْكُرْ اَخَا عَادٍ ؕ اِذْ اَنْذَرَ قَوْمَهٗ
بِالْاَحْقَافِ وَقَدْ خَلَتِ النُّذُرُ مِنْۢ بَيْنِ
يَدَيْهِ وَمِنْ خَلْفِهٖۤ اَلَّا تَعْبُدُوْۤا اِلَّا اللّٰهَ ؕ
اِنِّيْۤ اَخَافُ عَلَيْكُمْ عَذَابَ يَوْمٍ
عَظِيْمٍ ﴿٢١﴾

22. Na kumbuka nduguye 'Ad alipowaonya kaumu yake katika (nchi yenye) machuguu ya mchanga, na kwa yakini Waonyaji walitokea mbele yake na kabla yake: Msimwabudu ye yote ila Allah: hakika mimi nawahofieni adhabu ya siku iliyo kuu.

قَالُوْۤا اَجِئْتَنَا لِتَاْفِكَنَا عَنْ اٰلِهَتِنَا ۚ فَاْتِنَا
بِمَا تَعِدُنَاۤ اِنْ كُنْتَ مِنَ الصّٰدِقِيْنَ ﴿٢٢﴾

23. Wakasema: Je, umetujia ili utugeuze mbali na miungu yetu? Basi tuletee unayotuahidi ikiwa u miongoni mwa wasemao kweli.

قَالَ اِنَّمَا الْعِلْمُ عِنْدَ اللّٰهِ ۖ وَاُبَلِّغُكُمْ مَّاۤ
اُرْسِلْتُ بِهٖ وَلٰكِنِّيْۤ اَرٰىكُمْ قَوْمًا
تَجْهَلُوْنَ ﴿٢٣﴾

24. Akasema: Elimu hasa iko kwa Allah tu, nami ninawafikishieni yale niliyotumwa nayo, walakini ninawaoneni kuwa ninyi ni watu mfanyao ujinga.

فَلَمَّا رَاَوْهُ عَارِضًا مُّسْتَقْبِلَ اَوْدِيَتِهِمْ ۙ
قَالُوْا هٰذَا عَارِضٌ مُّمْطِرُنَا ؕ بَلْ هُوَ مَا
اسْتَعْجَلْتُمْ بِهٖ ؕ رِيْحٌ فِيْهَا عَذَابٌ اَلِيْمٌ ﴿٢٤﴾ ۙ

25. Basi walipoliona wingu likiyaelekea mabonde yao, wakasema: Wingu hili litatunyeshea mvua. Bali haya ni yale yale mliyokuwa mkiyaharakia kuyaomba: ni upepo wenye adhabu iumizayo,

تُدَمِّرُ كُلَّ شَيْءٍۭ بِاَمْرِ رَبِّهَا فَاَصْبَحُوْا
لَا يُرٰۤى اِلَّا مَسٰكِنُهُمْ ؕ كَذٰلِكَ
نَجْزِي الْقَوْمَ الْمُجْرِمِيْنَ ﴿٢٥﴾

26. Unaoangamiza kila kitu kwa amri ya Mola wake. Basi wamekuwa si wenye kuonekana ila maskani zao; hivyo ndivyo Tuwalipavyo watu wahalifu.

Aya 22. *Bil-Ahqaafi.* Neno hili linaweza kuwa na maana mbili: (1) *Katika (nchi yenye) machuguu ya mchanga,* yaani watu wa kabila la 'Ad walikuwa katika nchi yenye mchanga

وَلَقَدْ مَكَّنّٰهُمْ فِيْمَآ اِنْ مَّكَّنّٰكُمْ فِيْهِ وَجَعَلْنَا لَهُمْ سَمْعًا وَّاَبْصَارًا وَّاَفْـِٕدَةً ۖ فَمَآ اَغْنٰى عَنْهُمْ سَمْعُهُمْ وَلَآ اَبْصَارُهُمْ وَلَآ اَفْـِٕدَتُهُمْ مِّنْ شَيْءٍ اِذْ كَانُوْا يَجْحَدُوْنَ بِاٰيٰتِ اللّٰهِ وَحَاقَ بِهِمْ مَّا كَانُوْا بِهٖ يَسْتَهْزِءُوْنَ ﴿٢٦﴾ ع

27. Na bila shaka Tuliwastawisha katika yale Tusiyowastawisheni ninyi, na Tuliwapa masikio na macho na mioyo, lakini masikio yao na macho yao na mioyo yao havikuwafaa cho chote walipokuwa wakizikataa Aya za Allah na yakawazinga yale yale waliyoyafanyia mzaha.

FUNGU 4

وَلَقَدْ اَهْلَكْنَا مَا حَوْلَكُمْ مِّنَ الْقُرٰى وَصَرَّفْنَا الْاٰيٰتِ لَعَلَّهُمْ يَرْجِعُوْنَ ﴿٢٧﴾

28. Na hakika Tuliviangamiza pia vijiji vilivyowazungukeni na Tumezibainisha Ishara kwa namna namna ili wapate kurejea.

فَلَوْلَا نَصَرَهُمُ الَّذِيْنَ اتَّخَذُوْا مِنْ دُوْنِ اللّٰهِ قُرْبَانًا اٰلِهَةً ؕ بَلْ ضَلُّوْا عَنْهُمْ ۚ وَذٰلِكَ اِفْكُهُمْ وَمَا كَانُوْا يَفْتَرُوْنَ ﴿٢٨﴾

29. Basi mbona haikuwasaidia miungu ile waliyoishika kinyume cha Allah katika kupata ukaribu Naye? Bali imewapotea; na huo ndiyo uwongo wao na waliyokuwa wakiyatunga.

وَاِذْ صَرَفْنَآ اِلَيْكَ نَفَرًا مِّنَ الْجِنِّ يَسْتَمِعُوْنَ الْقُرْاٰنَ ۚ فَلَمَّا حَضَرُوْهُ قَالُوْٓا اَنْصِتُوْا ۚ فَلَمَّا قُضِيَ وَلَّوْا اِلٰى قَوْمِهِمْ مُّنْذِرِيْنَ ﴿٢٩﴾

30. Na Tulipokugeuzia kundi la majinni kwa kusikiliza Kurani; basi walipoihudhuria wakasema: Nyamazeni; na ilipokwisha (somwa) walirudi kwa jamaa zao wakiwaonya.

قَالُوْا يٰقَوْمَنَآ اِنَّا سَمِعْنَا كِتٰبًا اُنْزِلَ مِنْۢ بَعْدِ مُوْسٰى مُصَدِّقًا لِّمَا بَيْنَ يَدَيْهِ يَهْدِيْٓ اِلَى الْحَقِّ وَاِلٰى طَرِيْقٍ مُّسْتَقِيْمٍ ﴿٣٠﴾

31. Wakasema: Enyi watu wetu, hakika Tumekisikia Kitabu kilichoteremshwa baada ya Musa kinachosadikisha yaliyokuwa mbele yake, kinachoongoza kwenye haki na kwenye njia iliyonyooka.

---

mwingi; (2) aliwaonya *na machuguu ya mchanga,* ya kwamba machuguu yale ya mchanga ndiyo yatakayotumiwa kwa kuwaangamiza.

Aya 30. *Jinn* waliotajwa hapa ni wale wale Matajiri wa Kiyahudi wa Nasibin ambao walikuwa wakija Makka kufanya biashara, basi huko waliisikia Kurani wakaiamini (sura 72:7).

يٰقَوْمَنَآ اَجِيْبُوْا دَاعِيَ اللّٰهِ وَاٰمِنُوْا بِهٖ يَغْفِرْ لَكُمْ مِّنْ ذُنُوْبِكُمْ وَيُجِرْكُمْ مِّنْ عَذَابٍ اَلِيْمٍ ﴿٣٢﴾

32. Enyi watu wetu, mwitikieni Mwitaji wa Allah na mwaminini, Atawasameheni madhambi yenu na Atawalindeni na adhabu iumizayo.

وَمَنْ لَّا يُجِبْ دَاعِيَ اللّٰهِ فَلَيْسَ بِمُعْجِزٍ فِي الْاَرْضِ وَلَيْسَ لَهٗ مِنْ دُوْنِهٖٓ اَوْلِيَآءُ ؕ اُولٰٓئِكَ فِيْ ضَلٰلٍ مُّبِيْنٍ ﴿٣٣﴾

33. Na asiyemwitikia Mwitaji wa Allah, basi yeye hawezi kuwa mwenye kudhoofisha katika ardhi wala hatakuwa na walinzi badala yake. Hao wamo katika upotevu dhahiri.

اَوَلَمْ يَرَوْا اَنَّ اللّٰهَ الَّذِيْ خَلَقَ السَّمٰوٰتِ وَالْاَرْضَ وَلَمْ يَعْيَ بِخَلْقِهِنَّ بِقٰدِرٍ عَلٰٓى اَنْ يُّحْيِۦَ الْمَوْتٰى ؕ بَلٰٓى اِنَّهٗ عَلٰى كُلِّ شَيْءٍ قَدِيْرٌ ﴿٣٤﴾

34. Je, hawakuona ya kwamba Allah Aliyeziumba mbingu na ardhi na Hakuchoka katika kuziumba Ana uwezo wa kuwafufua wafu? Naam, hakika Yeye ni mweza wa kila kitu.

وَيَوْمَ يُعْرَضُ الَّذِيْنَ كَفَرُوْا عَلَى النَّارِ ؕ اَلَيْسَ هٰذَا بِالْحَقِّ ؕ قَالُوْا بَلٰى وَرَبِّنَا ؕ قَالَ فَذُوْقُوا الْعَذَابَ بِمَا كُنْتُمْ تَكْفُرُوْنَ ﴿٣٥﴾

35. Na siku watakayopelekwa wale waliokufuru Motoni; Je, hii si haki? Watasema: Naam! Wallahi (ni haki). Atasema: Basi onjeni adhabu kwa sababu mlikuwa mkikataa.

فَاصْبِرْ كَمَا صَبَرَ اُولُوا الْعَزْمِ مِنَ الرُّسُلِ وَلَا تَسْتَعْجِلْ لَّهُمْ ؕ كَاَنَّهُمْ يَوْمَ يَرَوْنَ مَا يُوْعَدُوْنَ ۙ لَمْ يَلْبَثُوْٓا اِلَّا سَاعَةً مِّنْ نَّهَارٍ ؕ بَلٰغٌ ۚ فَهَلْ يُهْلَكُ اِلَّا الْقَوْمُ الْفٰسِقُوْنَ ﴿٣٦﴾ ع

36. Basi subiri kama walivyosubiri Mitume wenye uimara, wala usiwaharakishie (adhabu). Siku watakayoyaona waliyoahidiwa itakuwa kana kwamba hawakukaa ila saa moja ya mchana. Huu ndiyo ufikisho! Basi hawataangamizwa ila watu wakosefu.

Aya 36. Mungu hana haraka na watu, maana anajua ya kuwa ingawa wamo katika raha na hawajali maonyo, lakini mara itakapowafikia adhabu inayokaa siku nyingi, basi raha yote itasahauliwa. Namna hii kwa adhabu ya siku Kiyama uchungu wake utawasahaulisha watu furaha zote walizoendesha, na wataona kama hawakupata kukaa hapa duniani ila saa moja tu.

سُوْرَةُ مُحَمَّدٍ مَّدَنِيَّةٌ وَّ هِيَ مَعَ الْبَسْمَلَةِ تِسْعٌ وَّ ثَلَاثُوْنَ اٰيَةً وَّ اَرْبَعَةُ رُكُوْعَاتٍ

47. SURA MUHAMMAD

Imeteremshwa Madina

Ina mafungu 4 na Aya 39 pamoja na Bismillahi

بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ ①

1. Kwa jina la Allah, Mwingi wa rehema, Mwingi wa ukarimu.

اَلَّذِيْنَ كَفَرُوْا وَصَدُّوْا عَنْ سَبِيْلِ اللّٰهِ اَضَلَّ اَعْمَالَهُمْ ②

2. Wale waliokufuru na wakawazuilia (watu) njia ya Allah, Ameviharibu vitendo vyao.

وَالَّذِيْنَ اٰمَنُوْا وَعَمِلُوا الصّٰلِحٰتِ وَاٰمَنُوْا بِمَا نُزِّلَ عَلٰى مُحَمَّدٍ وَّهُوَ الْحَقُّ مِنْ رَّبِّهِمْ ۙ كَفَّرَ عَنْهُمْ سَيِّاٰتِهِمْ وَاَصْلَحَ بَالَهُمْ ③

3. Na wale walioamini na wakatenda mema na wakaamini yaliyoteremshwa juu ya Muhammad, nayo ni haki iliyotoka kwa Mola wao, Atawafutia makosa yao na Atarekebisha hali yao.

ذٰلِكَ بِاَنَّ الَّذِيْنَ كَفَرُوا اتَّبَعُوا الْبَاطِلَ وَاَنَّ الَّذِيْنَ اٰمَنُوا اتَّبَعُوا الْحَقَّ مِنْ رَّبِّهِمْ ؕ كَذٰلِكَ يَضْرِبُ اللّٰهُ لِلنَّاسِ اَمْثَالَهُمْ ④

4. Hayo ni kwa sababu wale waliokufuru walifuata uongo, lakini wale walioamini wakafuata haki iliyotoka kwa Mola wao; hivi ndivyo Allah Huwapigia watu mifano yao.

Sura hii inaitwa *Muhammad* na pia inaitwa *Qitaal* (Vita), na ilishuka Madina. Jina la kwanza la sura hii linabashiria ya kuwa watu wanaomwamini Mtume Muhammad *s.a.w.* watapata mafanikio ya kidunia. Iliposhuka sura hii Waislamu walikuwa katika hali ya unyonge kabisa, na walikuwa wamekimbia kutoka majumba yao, na huko walikokimbilia wakawa katika hatari ya kufutwa kabisa na adui mwenye nguvu.

Jina la pili linabashiria ya kuwa adhabu waliyoahidiwa makafiri itawafikia katika namna ya vita na wakubwa wao wataangamia, wengine wao watatekwa au kushindwa na kudhalilika.

Aya 2. *Ataviharibu vitendo vyao,* yaani watu wanaofanya kazi ya kuwazuia watu wasiingine katika njia ya haki, kwa hakika wanasumbuka bure, maana, matokeo ya kazi yao hayatakuwa kama wanavyotaka, bali kweli ndiyo itakayoshinda.

Aya 3. Imani ina sharti mbili: (1) yakini; (2) utii. Hapo matendo mema lazima yatatokea katika imani yenye sharti hizo mbili. Imani ni kama mbegu na matendo mema ndiyo matunda yake. Basi kama mbegu haizai matunda haina maana, na imani pasipo matendo mema pia haina maana.

فَاِذَا لَقِيْتُمُ الَّذِيْنَ كَفَرُوْا فَضَرْبَ
الرِّقَابِ ؕ حَتّٰٓى اِذَآ اَثْخَنْتُمُوْهُمْ
فَشُدُّوا الْوَثَاقَ ۙ فَاِمَّا مَنًّۢا بَعْدُ وَاِمَّا
فِدَآءً حَتّٰى تَضَعَ الْحَرْبُ اَوْزَارَهَا ۚ
ذٰلِكَ ؕ وَلَوْ يَشَآءُ اللّٰهُ لَانْتَصَرَ مِنْهُمْ ۙ
وَلٰكِنْ لِّيَبْلُوَا۟ بَعْضَكُمْ بِبَعْضٍ ؕ وَالَّذِيْنَ
قُتِلُوْا فِيْ سَبِيْلِ اللّٰهِ فَلَنْ يُّضِلَّ
اَعْمَالَهُمْ ۝٥

5. Basi mnapokutana (vitani) na wale waliokufuru wapigeni shingo mpaka mmewashinda, kisha wafungeni sana, tena waacheni kwa ihsani au kwa kujikomboa, hata vita vitue mizigo yake. Ndivyo hivyo; na kama Allah Angalitaka Angalijilipiza kisasi kwao, lakini kusudio ni hili ili Awajaribu baadhi yenu kwa mikono ya wengine. Na wale waliouawa katika njia ya Allah basi Hataviharibu kamwe vitendo vyao.

سَيَهْدِيْهِمْ وَيُصْلِحُ بَالَهُمْ ۝٦

6. Atawaongoza na kuirekebisha hali yao.

وَيُدْخِلُهُمُ الْجَنَّةَ عَرَّفَهَا لَهُمْ ۝٧

7. Na Atawaingiza katika bustani Aliyoipamba na kuitunza kwa ajili yao.

يٰٓاَيُّهَا الَّذِيْنَ اٰمَنُوْٓا اِنْ تَنْصُرُوا اللّٰهَ
يَنْصُرْكُمْ وَيُثَبِّتْ اَقْدَامَكُمْ ۝٨

8. Enyi mlioamini, mkimsaidia Allah, Atawasaidieni na Ataiimarisha miguu yenu.

وَالَّذِيْنَ كَفَرُوْا فَتَعْسًا لَّهُمْ وَاَضَلَّ
اَعْمَالَهُمْ ۝٩

9. Na wale waliokufuru basi kwao ni maangamizo na Amevipoteza vitendo vyao.

ذٰلِكَ بِاَنَّهُمْ كَرِهُوْا مَآ اَنْزَلَ اللّٰهُ فَاَحْبَطَ
اَعْمَالَهُمْ ۝١٠

10. Hayo ni kwa sababu waliyachukia Aliyoyateremsha Allah, basi Akaviharibu vitendo vyao.

اَفَلَمْ يَسِيْرُوْا فِي الْاَرْضِ فَيَنْظُرُوْا
كَيْفَ كَانَ عَاقِبَةُ الَّذِيْنَ مِنْ قَبْلِهِمْ ؕ
دَمَّرَ اللّٰهُ عَلَيْهِمْ ۫ وَلِلْكٰفِرِيْنَ اَمْثَالُهَا ۝١١

11. Je, hawakutembea katika ardhi wakaona umekuwaje mwisho wa wale waliowatangulia? Allah Aliwaangamiza, na kwa makafiri itakuwa (adhabu) kama hii.

ذٰلِكَ بِاَنَّ اللّٰهَ مَوْلَى الَّذِيْنَ اٰمَنُوْا وَاَنَّ
الْكٰفِرِيْنَ لَا مَوْلٰى لَهُمْ ۝١٢ ع ١٢

12. Hayo ni kwa sababu Allah ni Mlinzi wa walioamini na kwa yakini makafiri hawana mlinzi.

Aya 5. Waislamu wanafunzwa na Aya hii ya kuwa mateka wakamatwe pale inapokuwa vita imepiganwa sana ili kupunguza nguvu ya adui. Na baadaye mateka hao wa vita wanaweza kusamehewa na kuachwa bure au wanaweza kujikomboa. Amri hii ya Kiislamu ingefumbua

FUNGU 2

13. Kwa hakika Allah Atawaingiza walioamini na wafanyao wema katika Bustani ipitayo mito ndani yake. Lakini waliokufuru hujifurahisha na hula kama walavyo wanyama, na Moto ni makao yao.

إِنَّ اللَّهَ يُدْخِلُ الَّذِينَ آمَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ جَنَّاتٍ تَجْرِي مِن تَحْتِهَا الْأَنْهَارُ ۖ وَالَّذِينَ كَفَرُوا يَتَمَتَّعُونَ وَيَأْكُلُونَ كَمَا تَأْكُلُ الْأَنْعَامُ وَالنَّارُ مَثْوًى لَّهُمْ ﴿١٢﴾

14. Na miji mingapi ilikuwa yenye nguvu zaidi kuliko mji wako (huu) unaokufukuza: Tuliwaangamiza wala hawakuwa na msaidizi.

وَكَأَيِّن مِّن قَرْيَةٍ هِيَ أَشَدُّ قُوَّةً مِّن قَرْيَتِكَ الَّتِي أَخْرَجَتْكَ ۚ أَهْلَكْنَاهُمْ فَلَا نَاصِرَ لَهُمْ ﴿١٣﴾

15. Je, mtu mwenye kuwa na dalili zitokazo kwa Mola wake atakuwa sawa na mtu aliyepambiwa ubaya wa matendo yake? Nao walifuata tamaa zao.

أَفَمَن كَانَ عَلَىٰ بَيِّنَةٍ مِّن رَّبِّهِ كَمَن زُيِّنَ لَهُ سُوءُ عَمَلِهِ وَاتَّبَعُوا أَهْوَاءَهُمْ ﴿١٤﴾

16. Mfano wa Pepo ile waliyoahidiwa watawa ni huu kwamba; imo mito ya maji yasiyoharibika asilan na mito ya maziwa yasiyobadilika ladha yake, na mito ya pombe yenye ladha kwa wanywao, na mito ya asali halisi; na humo watapata matunda ya kila namna na msamaha kutoka kwa Mola wao, basi je, hao watakuwa sawa na yule akaaye Motoni? na kunyweshwa maji yachemkayo yatakayokata matumbo yao?

مَّثَلُ الْجَنَّةِ الَّتِي وُعِدَ الْمُتَّقُونَ ۖ فِيهَا أَنْهَارٌ مِّن مَّاءٍ غَيْرِ آسِنٍ ۚ وَأَنْهَارٌ مِّن لَّبَنٍ لَّمْ يَتَغَيَّرْ طَعْمُهُ ۚ وَأَنْهَارٌ مِّنْ خَمْرٍ لَّذَّةٍ لِّلشَّارِبِينَ ۚ وَأَنْهَارٌ مِّنْ عَسَلٍ مُّصَفًّى ۖ وَلَهُمْ فِيهَا مِن كُلِّ الثَّمَرَاتِ وَمَغْفِرَةٌ مِّن رَّبِّهِمْ ۖ كَمَنْ هُوَ خَالِدٌ فِي النَّارِ وَسُقُوا مَاءً حَمِيمًا فَقَطَّعَ أَمْعَاءَهُمْ ﴿١٥﴾

---

macho ya wapinzani waisingiziao dini Ya Kiislamu kuwa inaruhusu wafuasi wake wapigane na watu wapate kuwaingiza katika dini au kuwashika mateka. Islam ni dini ya pekee yenye kuondoa utumwa duniani na kuwapa watu uhuru wa kushika dini yo yote waipendayo.

Aya 14. *Mji wako,* yaani Makka. Aya hii inaonyesha ya kwamba nguvu ya mji wa Makka itavunjika kama ilivyovunjika miji ya zamani. Na ndivyo ilivyotokea. Baadaye Mtume *s.a.w.* aliporudi Makka na wafuasi elfu kumi bila mapigano Makka ikatekwa, na maadui wakasamehewa, lakini nguvu waliyokuwa nayo ilikwisha, masanamu yakavunjwa, na Waislamu wakawa mabwana wa mji huo.

Aya 16. Aya hii inaonyesha ya kwamba neema zilizobainishwa katika Kurani kuwa malipo ya matendo ya waaminio ni mifano kwa kutufahamisha namna yao hapa duniani kadiri

17. Na wako miongoni mwao wanaokusikiliza, hata wanapoondoka kwako wanawauliza wale waliopewa elimu: (Mtume) amesema nini sasa? Hao ndio ambao Allah Amewapiga muhuri mioyoni mwao na wakafuata tamaa zao.

وَمِنْهُمْ مَّنْ يَّسْتَمِعُ اِلَيْكَ ۚ حَتّٰٓى اِذَا خَرَجُوْا مِنْ عِنْدِكَ قَالُوْا لِلَّذِيْنَ اُوْتُوا الْعِلْمَ مَاذَا قَالَ اٰنِفًا ۭ اُولٰۗىِٕكَ الَّذِيْنَ طَبَعَ اللّٰهُ عَلٰي قُلُوْبِهِمْ وَاتَّبَعُوْٓا اَهْوَاۗءَهُمْ ۝۱۷

18. Na wale walioongoka Amewazidishia mwongozo na Amewapa utawa wao.

وَالَّذِيْنَ اهْتَدَوْا زَادَهُمْ هُدًى وَّاٰتٰىهُمْ تَقْوٰىهُمْ ۝۱۸

19. Na hawangojei ila saa ile iwafikie kwa ghafla. Basi alama zake zimekwisha kuja. Hivyo (utawafaa) wapi ukumbusho wao itakapowafikia (saa)?

فَهَلْ يَنْظُرُوْنَ اِلَّا السَّاعَةَ اَنْ تَاْتِيَهُمْ بَغْتَةً ۚ فَقَدْ جَاۗءَ اَشْرَاطُهَا ۚ فَاَنّٰى لَهُمْ اِذَا جَاۗءَتْهُمْ ذِكْرٰىهُمْ ۝۱۹

20. Basi jua ya kwamba hakuna aabudiwaye ila Allah, na uombe ghofira kwa kuteleza kwako na kwa waaminio wanaume na waaminio wanawake. Na Allah Anajua mahali penu pa kurudia na mahali penu pa kukaa.

فَاعْلَمْ اَنَّهٗ لَآ اِلٰهَ اِلَّا اللّٰهُ وَاسْتَغْفِرْ لِذَنْۢبِكَ وَلِلْمُؤْمِنِيْنَ وَالْمُؤْمِنٰتِ ۭ وَاللّٰهُ يَعْلَمُ مُتَقَلَّبَكُمْ وَمَثْوٰىكُمْ ۝۲۰ ع

---

iwezekanavyo. Ijapokuwa katika Aya nyingi tumeahidiwa kupewa vitu vipatikanavyo ulimwenguni humu, lakini hivyo vinafanana na vile vya Akhera kwa majina tu. Hakika yao ni mbali kabisa hata mtu asiweze kuifahamu. Tazama sura 32:18.

Roho ya mtu ikiwa peke yake pasi na mwili wo wote haifanyi kitendo cho chote. Baada ya kuachana na mwili huu wa udongo usioweza kukaa milele, roho ya mtu itapewa mwili mpya wenye kuishi daima na utakaoweza kuzitumia neema za Peponi zidumuzo. Huko Peponi watu hawatachoka (sura 43:35). hali miili yetu hii huchoka. Neema za Peponi hazina kikomo (sura 13:36) hali vipawa vya dunia vitakwisha. Basi waaminio, huko Peponi, watakuwa na miili iliyo bora na myepesi kuliko hii ambayo wanayo sasa. Na neema watakazopewa zitakuwa za namna nyingine zenye kuifaa miili yao.

Waarabu husema "Usingizi ni ndugu ya mauti." Ndoto inaweza kueleza kidogo mambo ya Akhera. Katika ndoto mtu anajiona akisafiri au akitumia vyakula vya namna mbalimbali ingawa mwili wake hauondoki kitandani. Ndivyo mtu atajiona akivitumia vitu vingi vinavyofanana na vile vya dunia hii, baada ya kufa kwake. Mifereji ya maji na ya maziwa na ya asali na ya kileo imetajwa kuonyesha wingi wa hivyo vyote. Kileo cha Peponi hakilevyi kwa kutoa akili (sura 37:48). Kitawatakasa wanywaji (sura 76:22; 52:24).

FUNGU 3

وَيَقُوْلُ الَّذِيْنَ اٰمَنُوْا لَوْلَا نُزِّلَتْ سُوْرَةٌ ۚ فَاِذَآ اُنْزِلَتْ سُوْرَةٌ مُّحْكَمَةٌ وَّذُكِرَ فِيْهَا الْقِتَالُ ۙ رَاَيْتَ الَّذِيْنَ فِيْ قُلُوْبِهِمْ مَّرَضٌ يَّنْظُرُوْنَ اِلَيْكَ نَظَرَ الْمَغْشِيِّ عَلَيْهِ مِنَ الْمَوْتِ ۭ فَاَوْلٰى لَهُمْ ۝۲۰

21. Na walioamini husema: Mbona haijateremshwa Sura? Lakini inapokuwa inateremshwa Sura thabiti na ndani yake inatajwa vita, utawaona wale wenye maradhi katika mioyo yao wanakutazama mtazamo wa anayezimia kwa mauti. Basi ole wao!

طَاعَةٌ وَّقَوْلٌ مَّعْرُوْفٌ ۭ فَاِذَا عَزَمَ الْاَمْرُ ۭ فَلَوْ صَدَقُوا اللّٰهَ لَكَانَ خَيْرًا لَّهُمْ ۝۲۱

22. (Yanayotakiwa ni) utii na kauli njema; na amri inapoazimiwa, basi kama wakiwa wakweli kwa Allah bila shaka itakuwa bora kwao.

فَهَلْ عَسَيْتُمْ اِنْ تَوَلَّيْتُمْ اَنْ تُفْسِدُوْا فِي الْاَرْضِ وَتُقَطِّعُوْٓا اَرْحَامَكُمْ ۝۲۲

23. Je yawezekana kwenu kama mkipata utawala mfanye uharibifu ardhini na kuukata ujamaa wenu? (La hasha).

اُولٰۗىِٕكَ الَّذِيْنَ لَعَنَهُمُ اللّٰهُ فَاَصَمَّهُمْ وَاَعْمٰٓى اَبْصَارَهُمْ ۝۲۳

24. Hao ndio ambao Allah Amewalaani na Amewatia uziwi na Ameyapofusha macho yao.

اَفَلَا يَتَدَبَّرُوْنَ الْقُرْاٰنَ اَمْ عَلٰي قُلُوْبٍ اَقْفَالُهَا ۝۲۴

25. Je hawaitafakari Kurani, au mioyoni mwao mna kufuli zilizotengenezwa na mioyo yao?

اِنَّ الَّذِيْنَ ارْتَدُّوْا عَلٰٓي اَدْبَارِهِمْ مِّنْۢ بَعْدِ مَا تَبَيَّنَ لَهُمُ الْهُدَى ۙ الشَّيْطٰنُ سَوَّلَ لَهُمْ ۭ وَاَمْلٰى لَهُمْ ۝۲۵

26. Kwa hakika wale warudiao kwa migongo yao baada ya kuwabainikia mwongozo, Shetani amewafanyia vitendo vyao vionekane vizuri na kuwapa matumaini ya uongo.

ذٰلِكَ بِاَنَّهُمْ قَالُوْا لِلَّذِيْنَ كَرِهُوْا مَا نَزَّلَ اللّٰهُ سَنُطِيْعُكُمْ فِيْ بَعْضِ الْاَمْرِ ۚ وَاللّٰهُ يَعْلَمُ اِسْرَارَهُمْ ۝۲۶

27. Hayo ni kwa sababu wao waliwaambia wale walioyachukia yale Aliyoyateremsha Allah: Bila shaka tutakutiini katika baadhi ya mambo. Na Allah Anazijua siri zao.

فَكَيْفَ اِذَا تَوَفَّتْهُمُ الْمَلٰۗىِٕكَةُ يَضْرِبُوْنَ وُجُوْهَهُمْ وَاَدْبَارَهُمْ ۝۲۷

28. Basi itakuwaje Malaika watakapowafisha? Watawapiga nyuso zao na migongo yao.

ذٰلِكَ بِاَنَّهُمُ اتَّبَعُوْا مَآ اَسْخَطَ اللّٰهَ وَكَرِهُوْا رِضْوَانَهٗ فَاَحْبَطَ اَعْمَالَهُمْ ۝۲۸ ع ۳ ۷

29. Hayo ni kwa sababu wao waliyafuata yaliyomchukiza Allah na wakayachukia yanayomridhisha, basi Akaviharibu vitendo vyao.

FUNGU 4

30. Je, wale wenye maradhi mioyoni mwao walidhani kwamba Allah Hataidhihirisha bughudha yao?

اَمْ حَسِبَ الَّذِيْنَ فِيْ قُلُوْبِهِمْ مَّرَضٌ اَنْ لَّنْ يُّخْرِجَ اللّٰهُ اَضْغَانَهُمْ ﴿٣٠﴾

31. Na kama Tungependa Tungekuonesha hao na ungewatambua kwa alama zao; na hasa utawafahamu kwa namna ya usemi (wao); na Allah Anavijua vitendo vyenu.

وَلَوْ نَشَآءُ لَاَرَيْنٰكَهُمْ فَلَعَرَفْتَهُمْ بِسِيْمٰهُمْ ؕ وَلَتَعْرِفَنَّهُمْ فِيْ لَحْنِ الْقَوْلِ ؕ وَاللّٰهُ يَعْلَمُ اَعْمَالَكُمْ ﴿٣١﴾

32. Na bila shaka Tutawajaribuni mpaka Tuwapambanue wanaojitahidi kweli miongoni mwenu na wenye kusubiri, na Tubainishe hali zenu.

وَلَنَبْلُوَنَّكُمْ حَتّٰى نَعْلَمَ الْمُجٰهِدِيْنَ مِنْكُمْ وَالصّٰبِرِيْنَ ۙ وَنَبْلُوَاَخْبَارَكُمْ ﴿٣٢﴾

33. Kwa hakika wale waliokufuru na kuzuilia (watu) njia ya Allah na kupinzana na Mtume baada ya kuwabainikia mwongozo, wao hawamdhuru Allah cho chote, na punde Ataviharibu vitendo vyao.

اِنَّ الَّذِيْنَ كَفَرُوْا وَصَدُّوْا عَنْ سَبِيْلِ اللّٰهِ وَشَآقُّوا الرَّسُوْلَ مِنْۢ بَعْدِ مَا تَبَيَّنَ لَهُمُ الْهُدٰى ۙ لَنْ يَّضُرُّوا اللّٰهَ شَيْـًٔا ؕ وَسَيُحْبِطُ اَعْمَالَهُمْ ﴿٣٣﴾

34. Enyi mlioamini, Mtiini Allah na mtiini Mtume, na wala msiviharibu vitendo vyenu.

يٰۤاَيُّهَا الَّذِيْنَ اٰمَنُوْۤا اَطِيْعُوا اللّٰهَ وَاَطِيْعُوا الرَّسُوْلَ وَلَا تُبْطِلُوْۤا اَعْمَالَكُمْ ﴿٣٤﴾

35. Hakika wale waliokufuru na kuzuilia (watu) njia ya Allah kisha wakafa wakiwa ni makafiri, Allah Hatawasamehe kamwe.

اِنَّ الَّذِيْنَ كَفَرُوْا وَصَدُّوْا عَنْ سَبِيْلِ اللّٰهِ ثُمَّ مَاتُوْا وَهُمْ كُفَّارٌ فَلَنْ يَّغْفِرَ اللّٰهُ لَهُمْ ﴿٣٥﴾

36. Basi msilegee kuwaita kwenye suluhu wakati ninyi ndio mtakaoshinda. Na Allah Yu pamoja nanyi, na Hatawapunjeni malipo ya vitendo vyenu.

فَلَا تَهِنُوْا وَتَدْعُوْۤا اِلَى السَّلْمِ ۖۚ وَاَنْتُمُ الْاَعْلَوْنَ ۖۚ وَاللّٰهُ مَعَكُمْ وَلَنْ يَّتِرَكُمْ اَعْمَالَكُمْ ﴿٣٦﴾

Aya 36. Katika Aya zilizopita Allah ameeleza ya kwamba wanaokufuru hawatafanikiwa katika makusudi yao. Na katika Aya hii anawaambia Waislamu wasiingie uvivu

37. Hakika maisha ya dunia ni mchezo na upuuzi, na kama mkiamini na kujilinda, Atawapeni ujira wenu, wala Hatawaombeni mali zenu.

اِنَّمَا الْحَيٰوةُ الدُّنْيَا لَعِبٌ وَّ لَهْوٌ ؕ وَ اِنْ تُؤْمِنُوْا وَ تَتَّقُوْا يُؤْتِكُمْ اُجُوْرَكُمْ وَ لَا يَسْـَٔلْكُمْ اَمْوَالَكُمْ ﴿۳۷﴾

38. Kama Akiwaombeni hayo na kuwashurutisheni mtafanya ubahili; naye Ataitoa bughudha yenu.

اِنْ يَّسْـَٔلْكُمُوْهَا فَيُحْفِكُمْ تَبْخَلُوْا وَ يُخْرِجْ اَضْغَانَكُمْ ﴿۳۸﴾

39. Lo! ninyi ndio mnaitwa ili (mtoe) katika njia ya Allah, lakini wengine wenu wanafanya ubahili; na afanyaye ubahili basi hakika anafanya ubahili kwa (kuidhuru) nafsi yake. Na Allah ni Mkwasi nanyi ni mafakiri. Na kama mkirudi nyuma basi Ataleta watu wengine badala yenu, nao hawatakuwa mfano wenu.

هٰۤاَنْتُمْ هٰۤؤُلَآءِ تُدْعَوْنَ لِتُنْفِقُوْا فِيْ سَبِيْلِ اللّٰهِ ۚ فَمِنْكُمْ مَّنْ يَّبْخَلُ ۚ وَ مَنْ يَّبْخَلْ فَاِنَّمَا يَبْخَلُ عَنْ نَّفْسِهٖ ؕ وَ اللّٰهُ الْغَنِيُّ وَ اَنْتُمُ الْفُقَرَآءُ ۚ وَ اِنْ تَتَوَلَّوْا يَسْتَبْدِلْ قَوْمًا غَيْرَكُمْ ۙ ثُمَّ لَا يَكُوْنُوْۤا اَمْثَالَكُمْ ﴿۳۹﴾ ع

---

wa kueneza dini yao kwa kutumaini kuwa Mungu amekwisha waahidi kuwa makafiri watashindwa, maana mara watu wakiwa wavivu basi wanaweza kunyang'anywa haki zao kwa sababu ya ulegevu wao. Tena wanaambiwa hapa Waislamu wasiingie ulegevu na kutaka mapatano ya suluhu na adui, maana kufanya hivi ni kukubali kushindwa na kuzidisha ujeuri wa adui. Lakini kama adui anatuita kufanya suluhu basi ni lazima kukubali (sura 8:62).

Aya 37. Baadhi ya watu hutaka kuchanganyika na maadui ili wapate heshima ya dunia na hadhi na umaarufu. Wanaambiwa hapa ya kuwa maisha ya dunia kwa kuacha dini ni sawa na mchezo na upuuzi tu na ni kitu cha kupita. Njia ya salama ni kushika imani na utawa.

سُوْرَةُ الْفَتْحِ مَدَنِيَّةٌ وَّ هِيَ مَعَ الْبَسْمَلَةِ ثَلَا ثُوْنَ اٰيَةً وَّ اَرْبَعَةُ رُكُوْعَاتٍ

48. SURA AL-FAT'H

Imeteremshwa Madina

Ina mafungu 4 na Aya 30 pamoja na Bismillahi

بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ ①

1. Kwa jina la Allah, Mwingi wa rehema, Mwingi wa ukarimu.

اِنَّا فَتَحْنَا لَكَ فَتْحًا مُّبِيْنًا ②

2. Bila shaka Tumekupa ushindi ulio dhahiri,

لِّيَغْفِرَ لَكَ اللّٰهُ مَا تَقَدَّمَ مِنْ ذَنْۢبِكَ وَمَا تَاَخَّرَ وَيُتِمَّ نِعْمَتَهٗ عَلَيْكَ وَيَهْدِيَكَ صِرَاطًا مُّسْتَقِيْمًا ③

3. Ili Allah Akufunikie makosa yako (unayosingiziwa) yaliyotangulia na yajayo, na kukutimizia neema Yake na kukuongoza katika njia iliyonyooka.

Jina la sura hii limetoka katika Aya ya 2. Imeitwa *Ushindi* kwa sababu inaeleza habari za ushindi wa Waislamu ulioanzia Hudaibiyya na ambao umeendelea kushinda dini zote za dunia (Aya 29).

Seyidna Umar anasema ya kuwa Mtume *s.a.w.* alisoma sura hii kwa mara ya kwanza alipokuwa akirudi Madina kutoka Hudaibiyya (Bukhari); na hivyo tumejua ya kuwa ilishuka katika mwaka wa sita wa Hijra.

Aya 2. Ushindi huu unaotajwa hapa ni ule wa mkataba wa Hudaibiyya (Bukhari), ambao ingawa sharti zake hazikuwa zenye kupendeza kwa Waislamu, lakini walipata amani ya muda mrefu na wakaweza kuhubiri na kutangaza dini. Kadhalika watu wengine wakapata nafasi ya kusikia mafundisho ya Kiislamu na kuyachungua na wakaingia katika Uislamu kwa wingi. Hivyo mkataba huu wa Hudaibiyya ingawa kwa macho ya dhahiri ulionyesha kushindwa kwa Waislamu, lakini kwa hakika uliimarisha misingi ya kushindwa makafiri na kuushika mji wa Makka.

Aya 3. *Ghafara* maana yake ni kusitiri. Kughofiri dhambi za watu huwa kwa njia nyingi: (1) kutoadhibu mwenye dhambi na kumsamehe; (2) kuzifunika hata zisionekane na watu; (3) kuzuia dhambi zisitendeke; (4) kumhifadhi mtu asipate mawazo mabaya na kumlinda nyakati zote.

Akufunikie makosa yako. Mradi wake ni makosa ambayo makafiri na wanafiki walimsingizia nayo, kama kuzua uwongo juu ya Allah au kukosa katika matendo mengine.

Kushinda kwa Mtume *s.a.w.* kumeubatilisha upinzani wao kabisa. Nabii wa uwongo hapewi nafasi ya kuiimarisha dini yake na kuueneza uwongo wake siku nyingi. Kama mwenye kutunga uwongo vile vile angefanikiwa, ingekuwa shida kupambanua baina ya mkweli na mwongo. Mtume Muhammad *s.a.w.* hakuangamizwa kama manabii wa uwongo, bali wahalifu wake hasa ndio waliopondwa na *jiwe hili la pembeni* (Marko 12:10). Jambo hili lenyewe latosha kuyavunja-vunja maneno ya wampingao Mtume s.a.w. mpaka siku ya Kiyama.

Ni hatia kubwa kumwita Mtume Mtukufu *s.a.w.* mwenye dhambi. Aya hii pamoja na ile ifuatayo inaeleza maana ya kughofiri ni nini. Avunjaye amri za Allah, mbali na

وَّيَنْصُرَكَ اللّٰهُ نَصْرًا عَزِيْزًا ۝٤

4. Na Allah Akusaidie kwa msaada wenye nguvu.

هُوَ الَّذِيْٓ اَنْزَلَ السَّكِيْنَةَ فِيْ قُلُوْبِ الْمُؤْمِنِيْنَ لِيَزْدَادُوْٓا اِيْمَانًا مَّعَ اِيْمَانِهِمْ ؕ وَلِلّٰهِ جُنُوْدُ السَّمٰوٰتِ وَالْاَرْضِ ؕ وَكَانَ اللّٰهُ عَلِيْمًا حَكِيْمًا ۝٥

5. Yeye ndiye Aliyeteremsha utulivu katika mioyo ya waaminio ili waongeze-ke imani juu ya imani yao, na majeshi ya mbingu na ardhi ni ya Allah; na Allah ni Mwenye elimu, Mwenye hekima -

لِّيُدْخِلَ الْمُؤْمِنِيْنَ وَالْمُؤْمِنٰتِ جَنّٰتٍ تَجْرِيْ مِنْ تَحْتِهَا الْاَنْهٰرُ خٰلِدِيْنَ فِيْهَا وَيُكَفِّرَ عَنْهُمْ سَيِّاٰتِهِمْ ؕ وَكَانَ ذٰلِكَ عِنْدَ اللّٰهِ فَوْزًا عَظِيْمًا ۝٦

6. Ili Awaingize waaminio wanaume na waaminio wanawake katika Bustani ipitayo mito ndani yake wakae humo milele, na Awafutie makosa yao; na huo ndiyo ufaulu mkubwa mbele ya Allah.

وَّيُعَذِّبَ الْمُنٰفِقِيْنَ وَالْمُنٰفِقٰتِ وَالْمُشْرِكِيْنَ وَالْمُشْرِكٰتِ الظَّآنِّيْنَ بِاللّٰهِ ظَنَّ السَّوْءِ ؕ عَلَيْهِمْ دَآئِرَةُ السَّوْءِ ۚ وَغَضِبَ اللّٰهُ عَلَيْهِمْ وَلَعَنَهُمْ وَاَعَدَّ لَهُمْ جَهَنَّمَ ؕ وَسَآءَتْ مَصِيْرًا ۝٧

7. Na Awaadhibu wanafiki wanaume na wanafiki wanawake, na washirikina wanaume na washirikina wanawake, wanaomdhania Allah dhana mbaya; gurudumu la misiba litawazingira, na Allah Amewakasirikia na kuwalaani na kuwaandalia Jahanamu, nayo ni marudio mabaya.

kuishinda dunia na kupata neema iliyo timilifu, hufedheheshwa, Kurani inatangaza waziwazi ya kwamba Watumishi wa Allah hawapotezwi na Shetani (sura 15:43; 16:100; 17:66). Hasa wateule wachaguliwao kuwa Mitume wake wanahifadhiwa na shetani (sura 6:125). Mtume *s.a.w.* alisema, "Kila mtu anaye shetani ampotezaye na shetani wangu amepoa hata haniamuru ila wema." Maana kila mwanadamu tamaa yake inaweza kumkosesha, lakini yeye *s.a.w.* kwa maombi na ibada yake amepewa uwezo wa kujitawala na kumshinda shetani. Na zaidi ya hayo, aweza kuwaelekeza wenye dhambi kwenye njia ya wokofu. Wamfuatao Mtume *s.a.w.* hufanywa wapenzi wa Mungu (sura 3:32). Bali wanapewa cheo hata cha Unabii (sura 4:70). Mtume *s.a.w* ameitwa mwenye kuwatakasa watu (sura 62:3). Tena yu mfano mwema kwa ajili ya waaminio (sura 33:22).

Mtume *s.a.w.* aliomba ghofira kwa Allah siku zote. Kwa kuomba msamaha alitakasika na kutukuka zaidi kuliko watu wote. Usiku wa *Mi'iraaj* yeye alijiona amefika mahali ambapo hapakufika Mtume ye yote. Yeye mwenyewe alisema, Musa na Isa (amani ya Mungu juu yao) wangekuwa hai, wangalinifuata. Kuidumisha *istighfaar* ni ubora wa Mtume *s.a.w.* lakini ina-onekana aibu machoni pa makafiri. Maendeleo ya rohoni hayana mwisho na *istighfaar* ndiyo

وَلِلّٰهِ جُنُوْدُ السَّمٰوٰتِ وَالْاَرْضِ ؕ وَكَانَ اللّٰهُ عَزِيْزًا حَكِيْمًا ۝٨

8. Na majeshi ya mbingu na ardhi ni ya Allah, na Allah ni Mwenye ushindi kamili, Mwenye hekima.

اِنَّاۤ اَرْسَلْنٰكَ شَاهِدًا وَّ مُبَشِّرًا وَّنَذِيْرًا ۝٩

9. Hakika Tumekutuma uwe Shahidi na Mtoaji wa habari njema na Mwonyaji.

لِّتُؤْمِنُوْا بِاللّٰهِ وَرَسُوْلِهٖ وَتُعَزِّرُوْهُ وَتُوَقِّرُوْهُ ؕ وَ تُسَبِّحُوْهُ بُكْرَةً وَّ اَصِيْلًا ۝١٠

10. Ili Mumwamini Allah na Mtume Wake, na kumsaidia na kumheshimu na kumtukuza (Allah) asubuhi na jioni.

اِنَّ الَّذِيْنَ يُبَايِعُوْنَكَ اِنَّمَا يُبَايِعُوْنَ اللّٰهَ ؕ يَدُ اللّٰهِ فَوْقَ اَيْدِيْهِمْ ۚ فَمَنْ نَّكَثَ فَاِنَّمَا يَنْكُثُ عَلٰى نَفْسِهٖ ۚ وَمَنْ اَوْفٰى بِمَا عٰهَدَ عَلَيْهُ اللّٰهَ فَسَيُؤْتِيْهِ اَجْرًا عَظِيْمًا ۝١٠ ع

11. Bila shaka wanaofungamana nawe bila shaka wanafungamana na Allah. Mkono wa Allah uko juu ya mikono yao. Hivyo avunjaye, basi anavunja kwa kuidhuru nafsi yake tu; lakini atekelezaye aliyomwahidi Allah, basi Atamlipa ujira mkubwa.

FUNGU 2

سَيَقُوْلُ لَكَ الْمُخَلَّفُوْنَ مِنَ الْاَعْرَابِ شَغَلَتْنَاۤ اَمْوَالُنَا وَاَهْلُوْنَا فَاسْتَغْفِرْ لَنَا ۚ يَقُوْلُوْنَ بِاَلْسِنَتِهِمْ مَّا لَيْسَ فِيْ قُلُوْبِهِمْ ؕ قُلْ فَمَنْ يَّمْلِكُ لَكُمْ مِّنَ اللّٰهِ شَيْـًٔا

12. Karibuni watakuambia Mabedui wakaao nyuma: Mali zetu na ahali zetu vimetushughulisha, basi tuombee msamaha. Wanasema kwa ndimi zao yasiyokuwamo mioyoni mwao. Sema: Ni nani awezaye kuwasaidieni cho chote

---

Watu watakatifu kama Mitume hunyenyekea mbele ya Mola wao. Nabii Isa hakupenda hata kuitwa mwema (Luka 18:18), naye aliwafundisha wanafunzi wake kuomba, "Utusamehe dhambi zetu" na "Tuokoe na yule mwovu," (Luka 11:4).

Aya 11. *Mkono wa Allah uko juu ya mikono yao*. Mtume *s.a.w.* alipofunga ahadi na Masahaba wake alikuwa akishikana nao mikono. Sasa hapa mkono wa Mtume *s.a.w.* umeitwa mkono wa Mungu maana Manabii hawana nia katika vitendo vyao ila kama aamrishavyo Allah ndivyo wafanyayvo.

Aya 12. *Wakaao nyuma* ni watu amabao hawakutoka pamoja na Mtume *s.a.w.* kwa safari ya Hudaibiyya .

kwa Allah ikiwa Anataka kuwadhuruni au Anataka kuwanufaisheni? Bali Allah Anazo habari za mnayoyatenda.

اِنْ اَرَادَ بِكُمْ ضَرًّا اَوْ اَرَادَ بِكُمْ نَفْعًا ؕ
بَلْ كَانَ اللّٰهُ بِمَا تَعْمَلُوْنَ خَبِيْرًا ﴿۱۱﴾

13. Lakini mlidhani ya kwamba Mtume na waaminio hawatarudi kabisa kwa ahali zao, na mkapambwa hayo katika mioyo yenu, na mlidhani dhana mbaya, na mmekuwa watu waangamiao.

بَلْ ظَنَنْتُمْ اَنْ لَّنْ يَّنْقَلِبَ الرَّسُوْلُ
وَالْمُؤْمِنُوْنَ اِلٰٓى اَهْلِيْهِمْ اَبَدًا وَّزُيِّنَ ذٰلِكَ
فِىْ قُلُوْبِكُمْ وَظَنَنْتُمْ ظَنَّ السَّوْءِ ۖ
وَكُنْتُمْ قَوْمًۢا بُوْرًا ﴿۱۲﴾

14. Na asiyemwamini Allah na Mtume Wake, basi kwa hakika Tume-waandalia makafiri Moto uwakao.

وَمَنْ لَّمْ يُؤْمِنْۢ بِاللّٰهِ وَرَسُوْلِهٖ فَاِنَّآ
اَعْتَدْنَا لِلْكٰفِرِيْنَ سَعِيْرًا ﴿۱۳﴾

15. Na ufalme wa mbingu na ardhi ni wa Allah, Humsamehe Amtakaye na Humwadhibu Amtakaye, na Allah ni Msamehevu, Mrehemevu.

وَلِلّٰهِ مُلْكُ السَّمٰوٰتِ وَالْاَرْضِ ؕ يَغْفِرُ
لِمَنْ يَّشَآءُ وَيُعَذِّبُ مَنْ يَّشَآءُ ؕ وَكَانَ اللّٰهُ
غَفُوْرًا رَّحِيْمًا ﴿۱۴﴾

16. Karibuni watasema wale wakaao nyuma mtakapokwenda kuchukua mateka: Tuacheni tufuatane nanyi. Wanataka kuyabadili maneno ya Allah. Sema: Hamtatufuata kabisa, Allah Amekwisha sema hivi zamani! Ndipo watasema: bali ninyi mnatuhusudu. Siyo walikuwa hawafahamu ila kidogo!

سَيَقُوْلُ الْمُخَلَّفُوْنَ اِذَا انْطَلَقْتُمْ اِلٰى
مَغَانِمَ لِتَاْخُذُوْهَا ذَرُوْنَا نَتَّبِعْكُمْ ۚ
يُرِيْدُوْنَ اَنْ يُّبَدِّلُوْا كَلٰمَ اللّٰهِ ؕ قُلْ لَّنْ
تَتَّبِعُوْنَا كَذٰلِكُمْ قَالَ اللّٰهُ مِنْ قَبْلُ ۚ
فَسَيَقُوْلُوْنَ بَلْ تَحْسُدُوْنَنَا ؕ بَلْ كَانُوْا
لَا يَفْقَهُوْنَ اِلَّا قَلِيْلًا ﴿۱۵﴾

17. Waambie walioachwa nyuma katika watu wa jangwani: Karibuni mta-itwa kwa watu wenye mapigano makali, mtapigana nao au watasilimu, basi kama mkitii (Allah) Atawapeni ujira mzuri; na mkigeuka kama mlivyogeuka kwanza Atawaadhibuni adhabu iumizayo.

قُلْ لِّلْمُخَلَّفِيْنَ مِنَ الْاَعْرَابِ سَتُدْعَوْنَ
اِلٰى قَوْمٍ اُولِىْ بَاْسٍ شَدِيْدٍ تُقَاتِلُوْنَهُمْ
اَوْ يُسْلِمُوْنَ ۚ فَاِنْ تُطِيْعُوْا يُؤْتِكُمُ اللّٰهُ
اَجْرًا حَسَنًا ۚ وَاِنْ تَتَوَلَّوْا كَمَا تَوَلَّيْتُمْ
مِّنْ قَبْلُ يُعَذِّبْكُمْ عَذَابًا اَلِيْمًا ﴿۱۶﴾

18. Kipofu hana lawama wala kiwete hana lawama, wala mgonjwa hana lawama (wasipokwenda); na anayemtii Allah na Mtume Wake Atamwingiza ndani ya bustani zipitazo mito ndani yake; na atakayegeuka upande, Atamwadhibu adhabu iumizayo.

لَيْسَ عَلَى الْاَعْمٰى حَرَجٌ وَّلَا عَلَى
الْاَعْرَجِ حَرَجٌ وَّلَا عَلَى الْمَرِيْضِ
حَرَجٌ ؕ وَمَنْ يُّطِعِ اللّٰهَ وَرَسُوْلَهٗ يُدْخِلْهُ
جَنّٰتٍ تَجْرِيْ مِنْ تَحْتِهَا الْاَنْهٰرُ ۚ وَمَنْ
يَّتَوَلَّ يُعَذِّبْهُ عَذَابًا اَلِيْمًا ﴿۱۷﴾ ع

FUNGU 3

19. Kwa hakika Allah Amewawia radhi waaminio walipofungamana nawe chini ya mti, na Aliyajua yaliyomo mioyoni mwao. Basi Akateremsha utulivu juu yao, na Akawalipa ushindi wa karibu.

لَقَدْ رَضِيَ اللّٰهُ عَنِ الْمُؤْمِنِيْنَ اِذْ
يُبَايِعُوْنَكَ تَحْتَ الشَّجَرَةِ فَعَلِمَ مَا فِيْ
قُلُوْبِهِمْ فَاَنْزَلَ السَّكِيْنَةَ عَلَيْهِمْ
وَاَثَابَهُمْ فَتْحًا قَرِيْبًا ﴿۱۸﴾

20. Na mateka mengi watakayochukua; na Allah ni Mwenye ushindi kamili, Mwenye hekima.

وَّمَغَانِمَ كَثِيْرَةً يَّاْخُذُوْنَهَا ؕ وَكَانَ اللّٰهُ
عَزِيْزًا حَكِيْمًا ﴿۱۹﴾

21. Allah Amewaahidini mateka mengi mtakayoyachukua, kisha Akawahimizeni haya na Akaizuia mikono ya watu isiwafikieni, na ili iwe Ishara kwa waaminio na kuwaongozeni njia iliyonyooka.

وَعَدَكُمُ اللّٰهُ مَغَانِمَ كَثِيْرَةً تَاْخُذُوْنَهَا
فَعَجَّلَ لَكُمْ هٰذِهٖ وَكَفَّ اَيْدِيَ النَّاسِ
عَنْكُمْ ۚ وَلِتَكُوْنَ اٰيَةً لِّلْمُؤْمِنِيْنَ
وَيَهْدِيَكُمْ صِرَاطًا مُّسْتَقِيْمًا ﴿۲۰﴾

22. Na (ushindi) mwingine hamjaweza kuupata, (ambao) Allah Amekwisha uzingia, na Allah ni Mweza wa kila kitu.

وَّاُخْرٰى لَمْ تَقْدِرُوْا عَلَيْهَا قَدْ اَحَاطَ
اللّٰهُ بِهَا ؕ وَكَانَ اللّٰهُ عَلٰى كُلِّ شَيْءٍ قَدِيْرًا ﴿۲۱﴾

23. Na lau kama makafiri wangalipigana nanyi, bila shaka wangegeuza migongo, kisha wasingelipata mlinzi wala msaidizi.

وَلَوْ قٰتَلَكُمُ الَّذِيْنَ كَفَرُوْا لَوَلَّوُا
الْاَدْبَارَ ثُمَّ لَا يَجِدُوْنَ وَلِيًّا
وَّلَا نَصِيْرًا ﴿۲۲﴾

Aya 19. *Amewawia radhi.* Hawa wanaotajwa hapa ni Masahaba wapatao 1400 waliofunga ahadi pamoja Mtume *s.a.w*. chini ya mti huko Hudaibiyya.

Mtume *s.a.w.* alikuwa amefunga safari kwenda Makka kufanya Umra (Haji ndogo) pamoja na masahaba wake wapatao 1400. Makafiri walimzuia asiingie Makka. Kabla ya kuandikiana nao mkataba huo masahaba wake walifungamana naye ahadi kuwa watamlinda katika hali zote, hata watakufa wao mbele kabla hajauawa yeye. Ahadi hii ilifanywa chini ya mti (Bukhari). Mafungamano haya yanaitwa katika tareha ya Kiislamu *Bai'at-ur-Ridhwaan,* yaani mafungamano yaliyoridhiwa na Allah.

Aya 21. Aya hii inaeleza ushindi watakaoupata Waislamu baadaye ambao kushindwa kwa Makka pia kuko ndani yake.

سُنَّةَ اللّٰهِ الَّتِيْ قَدْ خَلَتْ مِنْ قَبْلُ ۚ وَلَنْ
تَجِدَ لِسُنَّةِ اللّٰهِ تَبْدِيْلًا ﴿٢٤﴾

24. Hiyo ndiyo kawaida ya Allah iliyotangulia zamani; wala hutapata mabadiliko katika kawaida ya Allah.

وَهُوَ الَّذِيْ كَفَّ اَيْدِيَهُمْ عَنْكُمْ
وَاَيْدِيَكُمْ عَنْهُمْ بِبَطْنِ مَكَّةَ مِنْۢ بَعْدِ
اَنْ اَظْفَرَكُمْ عَلَيْهِمْ ۭ وَكَانَ اللّٰهُ
بِمَا تَعْمَلُوْنَ بَصِيْرًا ﴿٢٥﴾

25. Na Yeye ndiye Aliyeizuia mikono yao kwenu, na mikono yenu kwao, katika bonde la Makka baada ya kuwapeni ushindi juu yao; na Allah ni Mwenye Kuyaona mnayoyatenda.

هُمُ الَّذِيْنَ كَفَرُوْا وَصَدُّوْكُمْ عَنِ
الْمَسْجِدِ الْحَرَامِ وَالْهَدْيَ مَعْكُوْفًا اَنْ يَّبْلُغَ
مَحِلَّهٗ ۭ وَلَوْلَا رِجَالٌ مُّؤْمِنُوْنَ وَنِسَاۗءٌ
مُّؤْمِنٰتٌ لَّمْ تَعْلَمُوْهُمْ اَنْ تَطَـــُٔوْهُمْ
فَتُصِيْبَكُمْ مِّنْهُمْ مَّعَرَّةٌۢ بِغَيْرِ عِلْمٍ ۚ
لِيُدْخِلَ اللّٰهُ فِيْ رَحْمَتِهٖ مَنْ يَّشَاۗءُ ۚ
لَوْ تَزَيَّلُوْا لَعَذَّبْنَا الَّذِيْنَ كَفَرُوْا مِنْهُمْ
عَذَابًا اَلِيْمًا ﴿٢٦﴾

26. Hao ndio waliokufuru na wakawazuilieni Msikiti Mtukufu, na dhabihu zikazuiliwa kufika mahali pao (pa kuchinjiwa); na lau kama si wanaume waaminio na wanawake waaminio msiowafahamu kwamba mtawakanyaga bila kujua, na kwahiyo mtapata masikitiko kwa ajili yao, (Mungu Asingewazuieni kupigana nao); ili Allah Amwingize Amtakaye katika rehema Yake. Kama (waaminio na makafiri) wangalitengana bila shaka Tungaliwaadhibu wale waliokufuru adhabu iumizayo.

اِذْ جَعَلَ الَّذِيْنَ كَفَرُوْا فِيْ قُلُوْبِهِمُ
الْحَمِيَّةَ حَمِيَّةَ الْجَاهِلِيَّةِ فَاَنْزَلَ اللّٰهُ
سَكِيْنَتَهٗ عَلٰي رَسُوْلِهٖ وَعَلَي الْمُؤْمِنِيْنَ
وَاَلْزَمَهُمْ كَلِمَةَ التَّقْوٰى وَكَانُوْٓا اَحَقَّ
بِهَا وَاَهْلَهَا ۭ وَكَانَ اللّٰهُ بِكُلِّ شَيْءٍ
عَلِيْمًا ﴿٢٦﴾ ع

27. Wale waliokufuru walipobeua mioyoni mwao ubeuzi wa kijinga, ndipo Allah Aliteremsha utulivu Wake juu ya Mtume Wake na juu ya waaminio, na Akawafanya wawe wenye kushikamana na neno la utawa, nao walikuwa ndio wenye haki zaidi nalo na waliostahili. Na Allah ni Mjuzi wa kila kitu.

FUNGU 4

لَقَدْ صَدَقَ اللّٰهُ رَسُوْلَهُ الرُّءْيَا بِالْحَقِّ ۚ
لَتَدْخُلُنَّ الْمَسْجِدَ الْحَرَامَ اِنْ شَاۗءَ اللّٰهُ
اٰمِنِيْنَ ۙ مُحَلِّقِيْنَ رُءُوْسَكُمْ

28. Kwa yakini Allah Amemhakikishia Mtume Wake njozi kwa haki: Bila shaka ninyi mtaingia katika Msikiti Mtukufu Inshaallah kwa

وَمُقَصِّرِيْنَ ۙ لَا تَخَافُوْنَ ؕ فَعَلِمَ مَا
لَمْ تَعْلَمُوْا فَجَعَلَ مِنْ دُوْنِ ذٰلِكَ
فَتْحًا قَرِيْبًا ﴿٢٨﴾

salama, mkinyoa vichwa vyenu na mkipunguza nywele, hamtaogopa, na (Allah) Alijua msiyoyajua, na kabla ya haya Aliwapeni ushindi ulio karibu.

هُوَ الَّذِيْٓ اَرْسَلَ رَسُوْلَهٗ بِالْهُدٰى
وَدِيْنِ الْحَقِّ لِيُظْهِرَهٗ عَلَى الدِّيْنِ كُلِّهٖ ؕ
وَكَفٰى بِاللّٰهِ شَهِيْدًا ﴿٢٩﴾

29. Yeye ndiye Aliyemtuma Mtume Wake kwa mwongozo na dini iliyo haki, ili Aishindishe juu ya dini zote; na Allah Hutosha kuwa Shahidi.

مُحَمَّدٌ رَّسُوْلُ اللّٰهِ ؕ وَالَّذِيْنَ مَعَهٗٓ
اَشِدَّآءُ عَلَى الْكُفَّارِ رُحَمَآءُ بَيْنَهُمْ
تَرٰىهُمْ رُكَّعًا سُجَّدًا يَّبْتَغُوْنَ فَضْلًا مِّنَ
اللّٰهِ وَرِضْوَانًا ۫ سِيْمَاهُمْ فِيْ وُجُوْهِهِمْ
مِّنْ اَثَرِ السُّجُوْدِ ؕ ذٰلِكَ مَثَلُهُمْ فِي
التَّوْرٰىةِ ۚۛ وَمَثَلُهُمْ فِي الْاِنْجِيْلِ ۚۛ
كَزَرْعٍ اَخْرَجَ شَطْئَهٗ فَاٰزَرَهٗ
فَاسْتَغْلَظَ فَاسْتَوٰى عَلٰى سُوْقِهٖ يُعْجِبُ
الزُّرَّاعَ لِيَغِيْظَ بِهِمُ الْكُفَّارَ ؕ وَعَدَ اللّٰهُ
الَّذِيْنَ اٰمَنُوْا وَعَمِلُوا الصّٰلِحٰتِ مِنْهُمْ
مَّغْفِرَةً وَّ اَجْرًا عَظِيْمًا ﴿٣٠﴾ ع ١٣

30. Muhammad ni Mtume wa Allah, na walio pamoja naye ni imara mbele ya makafiri na wenye kuhurumiana wao kwa wao; utawaona wakiinama na kusujudu, wakitafuta fadhili na ridhaa toka kwa Allah. Alama zao ni katika nyuso zao kwa athari ya kusujudu; huu ndiyo mfano wao katika Taurati na mfano wao katika Injili: kama mmea uliotoa chipuko, lake, kisha hulitia nguvu na ukavimba ndipo ukasimama sawa-sawa juu ya bua lake, ukawafurahisha wakulima ili Awakasirishe makafiri kwa ajili yao. Allah Amewaahidi walioamini na kutenda mema msamaha na ujira mkubwa.

Aya 28. Mtume *s.a.w.* alikuwa ameona ndoto ya kuwa yeye na masahaba wake wanafanya haji Makka. Basi ndiyo maana alifunga safari pamoja na kundi kubwa la masahaba wake. Lakini alipofika Hudaibiyya makafiri wakamzuia asiingie Makka kama tulivyokwisha eleza, naye akakubali kwa sharti ya kuwa atarudi kufanya haji mwakani. Seyidna Umar hakupendelea jambo hili na akamwambia Mtume *s.a.w.*, Utaachaje kuhiji nawe ueona ndoto unahiji? Mtume *s.a.w.* akamjibu ya kuwa, lakini sikuambiwa katika ndoto kuwa haji hii itafanywa mwaka gani. Basi ndoto hii ilisadikishwa na Mwenyezi Mungu na mwaka mwingine alikwenda Makka akahiji (Bukhari).

Katika habari hii kuna jambo moja linalotakiwa kukumbukwa. Manabii ni wanadamu tu, na pengine wanaweza kukosea kufahamu muradi hasa katika bishara za Allah, kama vile Mtume *s.a.w.* alivyokosea kufahamu muradi hasa katika ndoto yake.

سُوْرَةُ الْحُجُرَاتِ مَدَنِيَّةٌ وَّ هِيَ مَعَ الْبَسْمَلَةِ تِسْعَ عَشْرَةَ اٰيَةً وَّ رُكُوْعَانِ

49. SURA AL-HUJURAAT

Imeteremshwa Madina

Ina mafungu 2 na Aya 19 pamoja na Biismillahi

بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ ①

1. Kwa jina la Allah, Mwingi wa rehema, Mwingi wa ukarimu.

يٰۤاَيُّهَا الَّذِيْنَ اٰمَنُوْا لَا تُقَدِّمُوْا بَيْنَ يَدَيِ اللّٰهِ وَرَسُوْلِهٖ وَاتَّقُوا اللّٰهَ ؕ اِنَّ اللّٰهَ سَمِيْعٌ عَلِيْمٌ ②

2. Enyi mlioamini, msijitangulize mbele ya Allah na Mtume Wake, bali mcheni Allah. Hakika Allah ni Mwenye kusikia, Mwenye kujua.

يٰۤاَيُّهَا الَّذِيْنَ اٰمَنُوْا لَا تَرْفَعُوْۤا اَصْوَاتَكُمْ فَوْقَ صَوْتِ النَّبِيِّ وَلَا تَجْهَرُوْا لَهٗ بِالْقَوْلِ كَجَهْرِ بَعْضِكُمْ لِبَعْضٍ اَنْ تَحْبَطَ اَعْمَالُكُمْ وَاَنْتُمْ لَا تَشْعُرُوْنَ ③

3. Enyi mlioamini! msipaze sauti zenu kuliko sauti ya Nabii, wala msiseme naye kwa sauti kubwa kama mnavyosemezana ninyi kwa ninyi isije vitendo vyenu vikaharibika na hali hamtambui.

اِنَّ الَّذِيْنَ يَغُضُّوْنَ اَصْوَاتَهُمْ عِنْدَ رَسُوْلِ اللّٰهِ اُولٰٓئِكَ الَّذِيْنَ امْتَحَنَ اللّٰهُ قُلُوْبَهُمْ لِلتَّقْوٰى ؕ لَهُمْ مَّغْفِرَةٌ وَّاَجْرٌ عَظِيْمٌ ④

4. Kwa hakika wale wanaoshusha sauti zao mbele ya Mtume wa Allah, hao ndio ambao Allah Ameifanya mioyo yao kuwa ya utawa kwa njia ya majaribu. Wao watapata msamaha na ujira mkubwa.

اِنَّ الَّذِيْنَ يُنَادُوْنَكَ مِنْ وَّرَآءِ الْحُجُرٰتِ اَكْثَرُهُمْ لَا يَعْقِلُوْنَ ⑤

5. Kwa yakini wale wanaoanza kukuita (kwa sauti kubwa) wakiwa bado wako mbali na nyumba zako, wengi wao hawana akili.

Jina la sura hii linatoka katika Aya ya 5 ambayo inawafundisha waaminio wasimlalamikie Mtume *s.a.w.* anapokuwa faraghani nyumbani. Sura hii ilishuka wakati makundi ya watu yalipokuwa yakija kuingia Uislamu na hivyo ikatakikana kuwafundisha adabu nzuri.

Sura hii ilishuka Madina mwaka wa 9 wa Hijra.

Aya 2. Aya hii na zifuatazo zimeeleza namna ya adabu inayotakiwa kushikwa kwa ajili ya Mtume wa Mungu.

وَلَوْ اَنَّهُمْ صَبَرُوْا حَتّٰى تَخْرُجَ اِلَيْهِمْ لَكَانَ خَيْرًا لَّهُمْ ؕ وَاللّٰهُ غَفُوْرٌ رَّحِيْمٌ ۝٦

6. Na kama wangalingoja mpaka uwatokee, ingekuwa bora kwao. Na Allah ni Mwenye ghofira, Mwenye huruma.

يٰۤاَيُّهَا الَّذِيْنَ اٰمَنُوْۤا اِنْ جَآءَكُمْ فَاسِقٌۢ بِنَبَاٍ فَتَبَيَّنُوْۤا اَنْ تُصِيْبُوْا قَوْمًۢا بِجَهَالَةٍ فَتُصْبِحُوْا عَلٰى مَا فَعَلْتُمْ نٰدِمِيْنَ ۝٧

7. Enyi mlioamini! Kama fasiki akiwajieni na habari yo yote, basi pelelezeni, msije mkawadhuru watu kwa ujahili na mkawa wenye kujuta juu ya yale mliyoyatenda.

وَاعْلَمُوْۤا اَنَّ فِيْكُمْ رَسُوْلَ اللّٰهِ ؕ لَوْ يُطِيْعُكُمْ فِيْ كَثِيْرٍ مِّنَ الْاَمْرِ لَعَنِتُّمْ وَلٰكِنَّ اللّٰهَ حَبَّبَ اِلَيْكُمُ الْاِيْمَانَ وَزَيَّنَهٗ فِيْ قُلُوْبِكُمْ وَكَرَّهَ اِلَيْكُمُ الْكُفْرَ وَالْفُسُوْقَ وَالْعِصْيَانَ ؕ اُولٰٓئِكَ هُمُ الرّٰشِدُوْنَ ۝٨ۙ

8. Na jueni ya kwamba Mtume wa Allah yu kati yenu; lau yeye angewatiini katika mambo mengi bila shaka mngetaabika. Lakini Allah Ameipendezesha kwenu imani, na Ameipamba mioyoni mwenu, na Amewafanyeni muuchukie ukafiri na uovu na uasi. Hao ndio walioongoka,

فَضْلًا مِّنَ اللّٰهِ وَنِعْمَةً ؕ وَاللّٰهُ عَلِيْمٌ حَكِيْمٌ ۝٩

9. Kwa fadhili za Allah na neema Zake; na Allah ni Mwenye kujua, Mwenye hekima.

وَاِنْ طَآئِفَتٰنِ مِنَ الْمُؤْمِنِيْنَ اقْتَتَلُوْا فَاَصْلِحُوْا بَيْنَهُمَا ۚ فَاِنْۢ بَغَتْ اِحْدٰىهُمَا عَلَى الْاُخْرٰى فَقَاتِلُوا الَّتِيْ تَبْغِيْ حَتّٰى تَفِيْٓءَ اِلٰٓى اَمْرِ اللّٰهِ ۚ فَاِنْ فَآءَتْ فَاَصْلِحُوْا بَيْنَهُمَا بِالْعَدْلِ وَاَقْسِطُوْا ؕ اِنَّ اللّٰهَ يُحِبُّ الْمُقْسِطِيْنَ ۝١٠

10. Na ikiwa makundi mawili katika waaminio wanapigana, basi fanyeni suluhu kati yao; na ikiwa moja la hayo limeruka mipaka dhidi ya lingine, basi piganeni na lile lililoruka mpaka hadi lirudie kwenye uamuzi wa Allah. Na kama likirudi, basi yapatanisheni baina yao kwa uadilifu, na hukumuni kwa haki. Hakika Allah Huwapenda watendao haki.

اِنَّمَا الْمُؤْمِنُوْنَ اِخْوَةٌ فَاَصْلِحُوْا بَيْنَ اَخَوَيْكُمْ وَاتَّقُوا اللّٰهَ لَعَلَّكُمْ تُرْحَمُوْنَ ۝١١ ع

11. Kwa hakika waaminio ni ndugu, basi fanyeni suluhu baina ya ndugu zenu, na mcheni Allah ili mrehemiwe.

Aya 7. Aya hii inaeleza ya kuwa kama mtu asiye na mwendo mzuri katika dini alete habari juu ya mtu au watu, inatakiwa kwanza kuzipeleleza na kuona kama habari hizo ni sahihi au namna gani, isije ikakatwa shauri ya kuwadhuru watu bure.

Aya 10-11. Mara kunapotokea dalili za ugomvi kati ya mataifa mawili, mataifa

FUNGU 2

يٰٓاَيُّهَا الَّذِيْنَ اٰمَنُوْا لَا يَسْخَرْ قَوْمٌ مِّنْ قَوْمٍ عَسٰٓى اَنْ يَّكُوْنُوْا خَيْرًا مِّنْهُمْ وَلَا نِسَآءٌ مِّنْ نِّسَآءٍ عَسٰٓى اَنْ يَّكُنَّ خَيْرًا مِّنْهُنَّ ۚ وَلَا تَلْمِزُوْٓا اَنْفُسَكُمْ وَلَا تَنَابَزُوْا بِالْاَلْقَابِ ؕ بِئْسَ الِاسْمُ الْفُسُوْقُ بَعْدَ الْاِيْمَانِ ۚ وَمَنْ لَّمْ يَتُبْ فَاُولٰٓئِكَ هُمُ الظّٰلِمُوْنَ ⑪

12. Enyi mlioamini! Watu wasiwadhihaki watu wengine huenda wakawa ni bora kuliko wao; wala wanawake (wasiwadhihaki) wanawake huenda wakawa bora kuliko wao. Wala msisingiziane wala msiitane kwa majina mabaya. Ni jambo baya sana kujichumia sifa mbaya baada ya imani; na wale wasiotubu hao ndio wadhalimu.

يٰٓاَيُّهَا الَّذِيْنَ اٰمَنُوا اجْتَنِبُوْا كَثِيْرًا مِّنَ الظَّنِّ ۫ اِنَّ بَعْضَ الظَّنِّ اِثْمٌ وَّلَا تَجَسَّسُوْا وَلَا يَغْتَبْ بَّعْضُكُمْ بَعْضًا ؕ اَيُحِبُّ اَحَدُكُمْ اَنْ يَّاْكُلَ لَحْمَ اَخِيْهِ مَيْتًا فَكَرِهْتُمُوْهُ ؕ وَاتَّقُوا اللّٰهَ ؕ اِنَّ اللّٰهَ تَوَّابٌ رَّحِيْمٌ ⑫

13. Enyi mlioamini! Jiepusheni sana kufanya shuku, kwa hakika baadhi ya shuku ni dhambi, wala msipeleleze, wala baadhi yenu wasiwatete wengine; je, mmoja wenu anapenda kula nyama ya nduguye aliyekufa? La, hampendi: Na Mcheni Allah, bila shaka Allah ni Mwenye kupokea toba, Mrehemevu.

يٰٓاَيُّهَا النَّاسُ اِنَّا خَلَقْنٰكُمْ مِّنْ ذَكَرٍ وَّاُنْثٰى وَجَعَلْنٰكُمْ شُعُوْبًا وَّقَبَآئِلَ لِتَعَارَفُوْا ؕ اِنَّ اَكْرَمَكُمْ عِنْدَ اللّٰهِ اَتْقٰىكُمْ ؕ اِنَّ اللّٰهَ عَلِيْمٌ خَبِيْرٌ ⑬

14. Enyi watu! kwa hakika Tumewaumbeni katika kiume na kike, na Tumewafanyeni mataifa na makabila ili mjuane; hakika aheshimiwaye sana miongoni mwenu mbele ya Allah ni yule amchaye zaidi katika ninyi. Kwa yakini Allah ni Mjuzi, Mwenye habari.

mengine badala ya kusaidia taifa mojawapo, yawaite wagombanaji kuja patanishwa. Moja wapo likikataa kuja au kukataa uamuzi uliotolewa, mataifa yote yalichangie kulipiga vita mpaka litashindwa. Litakaposhindwa, yale mataifa mengine yaamue ugomvi ule wa kwanza, wala yasilete madai ya hasara zao, wala yasilihukumu kwa chuki kwa vile lilikataa amri yao kwanza, na lo lote lenye haki lipewe haki yake. Zaidi ya hayo hukumu iwe ya haki ili isilete mfundo unaoweza kuweka mbegu ya vita nyingine baadaye. Haya ndiyo mafundisho ya Kiislamu, yaliyoshuka wakati kabila la Aus na Khazraj wa Madina walipogombana, na ni ya namna ambayo kama yangefuatwa katika ulimwengu huu wa leo, amani kubwa ingeenea duniani, na vita vingepungua.

Aya 12-14. Katika Aya hizi mna maagizo ya kuwafanyia waaminio makao ya raha na kupendana. Taabu nyingi zinatokea kwa sababu ya kuacha maagizo haya. Katika Aya ya 14

قَالَتِ الْاَعْرَابُ اٰمَنَّا ؕ قُلْ لَّمْ تُؤْمِنُوْا
وَلٰكِنْ قُوْلُوْٓا اَسْلَمْنَا وَلَمَّا يَدْخُلِ
الْاِيْمَانُ فِيْ قُلُوْبِكُمْ ؕ وَاِنْ تُطِيْعُوا اللّٰهَ
وَرَسُوْلَهٗ لَا يَلِتْكُمْ مِّنْ اَعْمَالِكُمْ شَيْـًٔا ؕ
اِنَّ اللّٰهَ غَفُوْرٌ رَّحِيْمٌ ﴿١٥﴾

15. Walisema mabedui: Tumeamini. Sema: Hamjaamini, lakini semeni: Tumesilimu; maana imani haijaingia mioyoni mwenu; na mkimtii Allah na Mtume Wake, Hatapunguza cho chote katika vitendo vyenu. Kwa yakini Allah ni Msamehevu, Mrehemevu.

اِنَّمَا الْمُؤْمِنُوْنَ الَّذِيْنَ اٰمَنُوْا بِاللّٰهِ
وَرَسُوْلِهٖ ثُمَّ لَمْ يَرْتَابُوْا وَجٰهَدُوْا
بِاَمْوَالِهِمْ وَاَنْفُسِهِمْ فِيْ سَبِيْلِ اللّٰهِ ؕ
اُولٰٓئِكَ هُمُ الصّٰدِقُوْنَ ﴿١٦﴾

16. Hakika waaminio ni wale waliomwamini Allah na Mtume Wake, kisha wakawa si wenye kuona shaka na wakajitahidi kwa mali zao na nafsi zao katika njia ya Allah. Hao ndio wakweli.

قُلْ اَتُعَلِّمُوْنَ اللّٰهَ بِدِيْنِكُمْ ؕ وَاللّٰهُ يَعْلَمُ
مَا فِي السَّمٰوٰتِ وَمَا فِي الْاَرْضِ ؕ وَاللّٰهُ
بِكُلِّ شَيْءٍ عَلِيْمٌ ﴿١٧﴾

17. Sema: Je, mtamjulisha Allah dini yenu, na hali Allah Huyajua yaliyomo mbinguni na ardhini; na Allah ni Mjuzi wa kila kitu?

يَمُنُّوْنَ عَلَيْكَ اَنْ اَسْلَمُوْا ؕ قُلْ لَّا تَمُنُّوْا
عَلَيَّ اِسْلَامَكُمْ ۚ بَلِ اللّٰهُ يَمُنُّ عَلَيْكُمْ
اَنْ هَدٰىكُمْ لِلْاِيْمَانِ اِنْ كُنْتُمْ
صٰدِقِيْنَ ﴿١٨﴾

18. Wanafanya kwamba kusilimu kwao ni hisani kwako. Sema: Msionyeshe kwamba kusilimu kwenu ni kunifanyia hisani. Bali ni Allah Anayewafanyieni hisani kwa kuwaongozeni kwenye imani iwapo ninyi ni wakweli.

اِنَّ اللّٰهَ يَعْلَمُ غَيْبَ السَّمٰوٰتِ
وَالْاَرْضِ ؕ وَاللّٰهُ بَصِيْرٌ بِمَا تَعْمَلُوْنَ ﴿١٩﴾ ع ١٤

19. Bila shaka Allah Huzijua ghaibu za mbinguni na ardhini; na Allah Huyaona mnayoyatenda.

---

inasemwa, *Tumewafanyeni mataifa na makabila ili mjuane, hakika aheshimiwaye sana miongoni mwenu mbele ya Allah ni yule amchaye zaidi katika ninyi.* Fundisho hili linavunja kabisa ubora wa rangi na kabila, na limewawekea watu ubora hasa wanaotakiwa kuushindania, nao ni kufanya bidii kumcha Mungu na kumtii. Ama *kuteta* ni kumsema mtu kwa maneno ambayo usingeyasema kama angekuwapo na yatamchukiza kama akiyasikia. Kuteta ni dhambi kubwa kabisa inayovunja ujamaa na kuwatia watu katika uadui mkubwa. Mungu amesema kumteta mtu ni kama mtu kula nyama ya nduguye aliyekufa.

سُوْرَةُ قٓ مَكِّيَّةٌ وَّ هِيَ مَعَ الْبَسْمَلَةِ سِتٌّ وَّ اَرْبَعُوْنَ اٰيَةً وَّ ثَلَاثَةُ رُكُوْعَاتٍ

50. SURA QAAF

Imeteremshwa Makka

Ina mafungu 3 na Aya 46 pamoja na Bismillahi

بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ ①

1. Kwa jina la Allah, Mwingi wa rehema, Mwingi wa ukarimu.

قٓ ۚ وَالْقُرْاٰنِ الْمَجِيْدِ ۚ ②

2. (Allah) Mwenye nguvu. Naapa kwa Kurani Tukufu.

بَلْ عَجِبُوْٓا اَنْ جَآءَهُمْ مُّنْذِرٌ مِّنْهُمْ فَقَالَ الْكٰفِرُوْنَ هٰذَا شَيْءٌ عَجِيْبٌ ۚ ③

3. Bali wanastaajabu ya kwamba amewafikia Mwonyaji kutoka miongoni mwao, na wakasema makafiri: Hili ni jambo la ajabu!

ءَاِذَا مِتْنَا وَكُنَّا تُرَابًا ۚ ذٰلِكَ رَجْعٌۢ بَعِيْدٌ ④

4. Je! tutakapokufa na kuwa udongo? Marudio hayo ni ya mbali.

قَدْ عَلِمْنَا مَا تَنْقُصُ الْاَرْضُ مِنْهُمْ ۚ وَعِنْدَنَا كِتٰبٌ حَفِيْظٌ ⑤

5. Kwa hakika Tunajua yale ardhi inayowapunguzia, na Kwetu kiko Kitabu kinachohifadhi.

بَلْ كَذَّبُوْا بِالْحَقِّ لَمَّا جَآءَهُمْ فَهُمْ فِيْٓ اَمْرٍ مَّرِيْجٍ ⑥

6. Lakini waliikadhibisha haki ilipowafikia, na wamo katika jambo lihangaishalo.

اَفَلَمْ يَنْظُرُوْٓا اِلَى السَّمَآءِ فَوْقَهُمْ كَيْفَ بَنَيْنٰهَا وَزَيَّنّٰهَا وَمَا لَهَا مِنْ فُرُوْجٍ ⑦

7. Je, hawazitazami mbingu zilizo juu yao Tumezijengaje na Tumezipambaje wala hazina nyufa?

وَالْاَرْضَ مَدَدْنٰهَا وَاَلْقَيْنَا فِيْهَا رَوَاسِيَ وَاَنْۢبَتْنَا فِيْهَا مِنْ كُلِّ زَوْجٍۢ بَهِيْجٍ ⑧

8. Na ardhi Tumeitandaza na Tukaiwekea milima na Tukaimeesha mimea mizuri ya kila namna.

Sura hii imepewa jina la herufi ya mkato *Qaaf* inayotokea mwanzo wa Aya ya 2. Sura hii inakubaliwa na wote kuwa ilishuka Makka.

Aya 2. *Qaaf* ni herufi ya mkato kwa ajili ya sifa ya Allah iitwayo *Qadiir* yaani Mwenye nguvu, Mwenye uwezo na Mwenye Kudra.

Naapa kwa Kurani iliyo tukufu. Kiapo ni namna ya ushahidi. Na Allah kuapa kwa Kurani muradi wake ni kwamba anaitoa Kurani hii kuwa shahidi juu ya Kudra Yake na uwezo Wake.

تَبْصِرَةً وَّذِكْرٰى لِكُلِّ عَبْدٍ مُّنِيْبٍ ۝٩

9. Ni busara na ukumbusho kwa kila mtu arejeae mara kwa mara kwa Allah.

وَنَزَّلْنَا مِنَ السَّمَآءِ مَآءً مُّبٰرَكًا فَاَنْۢبَتْنَا بِهٖ جَنّٰتٍ وَّحَبَّ الْحَصِيْدِ ۝٩

10. Na Tumeyateremsha kutoka mawinguni maji yaliyobarikiwa, na kwayo Tukameesha mabustani na nafaka ivunwayo.

وَالنَّخْلَ بٰسِقٰتٍ لَّهَا طَلْعٌ نَّضِيْدٌ ۝١١

11. Na mitende mirefu yenye makole yapambayo kochokocho:

رِّزْقًا لِّلْعِبَادِ ۙ وَاَحْيَيْنَا بِهٖ بَلْدَةً مَّيْتًا ؕ كَذٰلِكَ الْخُرُوْجُ ۝١٢

12. Riziki kwa ajili ya watu, na (kutokana na mvua) Tukaufufua mji uliokufa; ndivyo ulivyo ufufuo.

كَذَّبَتْ قَبْلَهُمْ قَوْمُ نُوْحٍ وَّاَصْحٰبُ الرَّسِّ وَثَمُوْدُ ۝١٣

13. Walikadhibisha kabla yao watu wa Nuhu na wachimba madini na Wathamudi,

وَعَادٌ وَّفِرْعَوْنُ وَاِخْوَانُ لُوْطٍ ۝١٤

14. Na Waadi na Firauni na nduguze Luti,

وَّاَصْحٰبُ الْاَيْكَةِ وَقَوْمُ تُبَّعٍ ؕ كُلٌّ كَذَّبَ الرُّسُلَ فَحَقَّ وَعِيْدِ ۝١٥

15. Na waishio ndani ya misitu yenye miti mingi na watu wa Tubba; wote waliwakadhibisha Mitume, kwa hiyo onyo Langu likathibitika.

اَفَعَيِيْنَا بِالْخَلْقِ الْاَوَّلِ ؕ بَلْ هُمْ فِيْ لَبْسٍ مِّنْ خَلْقٍ جَدِيْدٍ ۝١٦ ع ١

16. Je, Tumechoka na uumbaji wa kwanza? Bali wao wamo katika shaka juu ya uumbaji mpya.

FUNGU 2

وَلَقَدْ خَلَقْنَا الْاِنْسَانَ وَنَعْلَمُ مَا تُوَسْوِسُ بِهٖ نَفْسُهٗ ۚ وَنَحْنُ اَقْرَبُ اِلَيْهِ مِنْ حَبْلِ الْوَرِيْدِ ۝١٧

17. Na bila shaka Tumemwumba mtu nasi Tunajua wasiwasi inaomtia nafsi yake, nasi Tu karibu naye zaidi kuliko hata halkumu (yake).

اِذْ يَتَلَقَّى الْمُتَلَقِّيٰنِ عَنِ الْيَمِيْنِ وَعَنِ الشِّمَالِ قَعِيْدٌ ۝١٨

18. Wanapopokea wapokeaji wawili, wakikaa kuume na kushoto.

مَا يَلْفِظُ مِنْ قَوْلٍ اِلَّا لَدَيْهِ رَقِيْبٌ عَتِيْدٌ ۝١٩

19. Hatoi kauli yo yote, isipokuwa karibu naye yuko mngojeaji tayari (kuandika).

وَجَآءَتْ سَكْرَةُ الْمَوْتِ بِالْحَقِّ ؕ ذٰلِكَ مَا كُنْتَ مِنْهُ تَحِيْدُ ۝٢٠

20. Na sakara ya mauti itakuja kwa haki: hayo ndiyo uliyotaka kujiepusha nayo.

Aya 18. *Kuume* yaani kwenye mema; na *kushoto* ni kwenye maovu (Taj).

وَنُفِخَ فِي الصُّوْرِ ؕ ذٰلِكَ يَوْمُ الْوَعِيْدِ ﴿٢١﴾

21. Na itapulizwa parapanda: hiyo ndiyo siku ya miadi.

وَجَآءَتْ كُلُّ نَفْسٍ مَّعَهَا سَآئِقٌ وَّشَهِيْدٌ ﴿٢٢﴾

22. Na itakuja kila nafsi pamoja na mwendeshaji na shahidi.

لَقَدْ كُنْتَ فِيْ غَفْلَةٍ مِّنْ هٰذَا فَكَشَفْنَا عَنْكَ غِطَآءَكَ فَبَصَرُكَ الْيَوْمَ حَدِيْدٌ ﴿٢٣﴾

23. Kwa hakika ulikuwa huna habari ya jambo hili, lakini Tumekuondolea pazia lako na macho yako leo yamekuwa makali.

وَقَالَ قَرِيْنُهٗ هٰذَا مَا لَدَيَّ عَتِيْدٌ ؕ ﴿٢٤﴾

24. Na mwenzake atamwambia: Hayo ndiyo yaliyowekwa tayari kwangu.

اَلْقِيَا فِيْ جَهَنَّمَ كُلَّ كَفَّارٍ عَنِيْدٍ ۙ ﴿٢٥﴾

25. Mtupeni katika Jahanamu kila kafiri asi,

مَّنَّاعٍ لِّلْخَيْرِ مُعْتَدٍ مُّرِيْبِ ۙ ﴿٢٦﴾

26. Akatazaye heri, arukaye mipaka, ashukuye,

الَّذِيْ جَعَلَ مَعَ اللّٰهِ اِلٰهًا اٰخَرَ فَاَلْقِيٰهُ فِي الْعَذَابِ الشَّدِيْدِ ﴿٢٧﴾

27. Aliyeweka mungu mwingine pamoja na Allah, basi mtupeni katika adhabu kali.

قَالَ قَرِيْنُهٗ رَبَّنَا مَآ اَطْغَيْتُهٗ وَلٰكِنْ كَانَ فِيْ ضَلٰلٍ بَعِيْدٍ ﴿٢٨﴾

28. Mwenzake atasema, Ee Mola wetu, sikumpotosha, bali yeye alikuwa katika upotevu wa mbali.

قَالَ لَا تَخْتَصِمُوْا لَدَيَّ وَقَدْ قَدَّمْتُ اِلَيْكُمْ بِالْوَعِيْدِ ﴿٢٩﴾

29. Atasema: Msihusumiane mbele Yangu, Nilikwisha watangulizieni onyo.

مَا يُبَدَّلُ الْقَوْلُ لَدَيَّ وَمَآ اَنَا بِظَلَّامٍ لِّلْعَبِيْدِ ﴿٣٠﴾ ع ٢

30. Kwangu kauli haibadilishwi, wala Mimi Siwadhulumu watumishi.

FUNGU 3

يَوْمَ نَقُوْلُ لِجَهَنَّمَ هَلِ امْتَلَاْتِ وَتَقُوْلُ هَلْ مِنْ مَّزِيْدٍ ﴿٣١﴾

31. Siku Tutakayoiambia Jahanamu: Je, umejaa? Nayo itasema: Je, kuna zaidi?

وَاُزْلِفَتِ الْجَنَّةُ لِلْمُتَّقِيْنَ غَيْرَ بَعِيْدٍ ﴿٣٢﴾

32. Na Pepo italetwa karibu, kwa wamchao Mungu bila ya kuwa mbali.

هٰذَا مَا تُوْعَدُوْنَ لِكُلِّ اَوَّابٍ حَفِيْظٍ ۚ ﴿٣٣﴾

33. Hiyo ndiyo mnayoahidiwa, kwa kila aelekeaye, ajilindaye;

مَنْ خَشِيَ الرَّحْمٰنَ بِالْغَيْبِ وَجَآءَ بِقَلْبٍ مُّنِيْبِ ۙ ﴿٣٤﴾

34. Anayemwogopa Rahmani faraghani na akaja kwa moyo uelekeao:

ادْخُلُوْهَا بِسَلٰمٍ ؕ ذٰلِكَ يَوْمُ الْخُلُوْدِ ﴿٣٥﴾

35. Iingieni kwa salama, hii ndio siku ya kuishi milele.

لَهُمْ مَّا يَشَآءُوْنَ فِيْهَا وَلَدَيْنَا مَزِيْدٌ ﴿٣٥﴾

36. Humo watapata cho chote wakitakacho; na Kwetu kuna zaidi.

وَكَمْ اَهْلَكْنَا قَبْلَهُمْ مِّنْ قَرْنٍ هُمْ اَشَدُّ مِنْهُمْ بَطْشًا فَنَقَّبُوْا فِى الْبِلَادِ ؕ هَلْ مِنْ مَّحِيْصٍ ﴿٣٦﴾

37. Na vizazi vingapi Tumevianga-miza kabla yao waliokuwa na nguvu zaidi kuliko hawa, nao walitengeneza mapango ardhini; je lipo kimbilio?

اِنَّ فِىْ ذٰلِكَ لَذِكْرٰى لِمَنْ كَانَ لَهٗ قَلْبٌ اَوْ اَلْقَى السَّمْعَ وَهُوَ شَهِيْدٌ ﴿٣٧﴾

38. Kwa yakini katika jambo hili mna ukumbusho kwa mwenye moyo au kwa ategaye sikio naye mwenyewe yu shahidi.

وَلَقَدْ خَلَقْنَا السَّمٰوٰتِ وَالْاَرْضَ وَمَا بَيْنَهُمَا فِىْ سِتَّةِ اَيَّامٍ ۖ وَّمَا مَسَّنَا مِنْ لُّغُوْبٍ ﴿٣٨﴾

39. Na bila shaka Tumeziumba mbingu na ardhi na vilivyomo kati yao katika nyakati sita, wala uchovu haukutugusa.

فَاصْبِرْ عَلٰى مَا يَقُوْلُوْنَ وَسَبِّحْ بِحَمْدِ رَبِّكَ قَبْلَ طُلُوْعِ الشَّمْسِ وَقَبْلَ الْغُرُوْبِ ﴿٣٩﴾ ۚ

40. Basi vumilia hayo wasemayo na Mtukuze Mola wako kwa kumsifu kabla ya kutoka jua na kabla ya kuchwa.

وَمِنَ الَّيْلِ فَسَبِّحْهُ وَاَدْبَارَ السُّجُوْدِ ﴿٤٠﴾

41. Na katika usiku Mtukuze na pia baada ya kusujudu.

وَاسْتَمِعْ يَوْمَ يُنَادِ الْمُنَادِ مِنْ مَّكَانٍ قَرِيْبٍ ﴿٤١﴾ ۙ

42. Na sikia Siku atakayonadi mnadi toka mahali pa karibu.

يَّوْمَ يَسْمَعُوْنَ الصَّيْحَةَ بِالْحَقِّ ؕ ذٰلِكَ يَوْمُ الْخُرُوْجِ ﴿٤٢﴾

43. Siku ambapo bila shaka yo yote watausikia mngurumo, hiyo ndiyo Siku ya kutoka.

اِنَّا نَحْنُ نُحْىٖ وَنُمِيْتُ وَاِلَيْنَا الْمَصِيْرُ ﴿٤٣﴾ ۙ

44. Bila shaka Sisi Tunahuisha na Tunafisha, na marudio ni Kwetu.

يَوْمَ تَشَقَّقُ الْاَرْضُ عَنْهُمْ سِرَاعًا ؕ ذٰلِكَ حَشْرٌ عَلَيْنَا يَسِيْرٌ ﴿٤٤﴾

45. Siku itakapowapasukia ardhi kutokana na mwendo wake wa kasi; huo ni mkusanyo rahisi Kwetu.

نَحْنُ اَعْلَمُ بِمَا يَقُوْلُوْنَ وَمَآ اَنْتَ عَلَيْهِمْ بِجَبَّارٍ ۘ فَذَكِّرْ بِالْقُرْاٰنِ مَنْ يَّخَافُ وَعِيْدِ ﴿٤٥﴾ ع ١٦ ١٧

46. Sisi Tunajua sana wanayoyasema, wala wewe si msimamizi wao wa kuwasuluhisha kwa nguvu; kwa hiyo umkumbushe kwa Kurani anayeogopa onyo Langu.

Aya 39. *Wala uchovu haukutugusa.* Biblia inasema Mungu alipumzika siku ya saba (Kutoka 20:11). Lakini Kurani inasema, Mungu hachoki. Basi asiyechoka alipumzikaje? Tazameni jinsi Kurani inavyodhihirisha heshima Ya Allah, na jinsi Biblia inavyoivunja!

سُوْرَةُ الذّٰرِيٰتِ مَكِّيَّةٌ وَّ هِيَ مَعَ الْبَسْمَلَةِ اِحْدٰى وَ سِتُّوْنَ اٰيَةً وَّ ثَلَاثَةُ رُكُوْعَاتٍ

51. SURA ADH-DHAARIYAAT

Imeteremshwa Makka

Ina mafungu 3 na Aya 61 pamoja na Bismillahi

بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ ①

1. Kwa jina la Allah, Mwingi wa rehema, Mwingi wa ukarimu.

وَالذّٰرِيٰتِ ذَرْوًا ②

2. Naapa kwa watawanyao sana.

فَالْحٰمِلٰتِ وِقْرًا ③

3. Tena kwa wabebao mzigo,

فَالْجٰرِيٰتِ يُسْرًا ④

4. Na kwa waendao kwa wepesi,

فَالْمُقَسِّمٰتِ اَمْرًا ⑤

5. Kisha kwa wagawanyao amri,

اِنَّمَا تُوْعَدُوْنَ لَصَادِقٌ ⑥

6. Bila shaka mnayoahidiwa ndio ya kweli,

وَّ اِنَّ الدِّيْنَ لَوَاقِعٌ ⑦

7. Na kwa hakika siku ya malipo bila shaka itatokea.

وَالسَّمَآءِ ذَاتِ الْحُبُكِ ⑧

8. Naapa kwa mbingu zenye njia,

اِنَّكُمْ لَفِيْ قَوْلٍ مُّخْتَلِفٍ ⑨

9. Kwa hakika ninyi mko katika kauli inayohitilafiana.

يُّؤْفَكُ عَنْهُ مَنْ اُفِكَ ⑩

10. Atageuzwa mbali na ukweli ulioahidiwa yule tu mwenye sifa za kugeuzwa mbali.

قُتِلَ الْخَرّٰصُوْنَ ⑪

11. Wazushi wameangamizwa.

الَّذِيْنَ هُمْ فِيْ غَمْرَةٍ سَاهُوْنَ ⑫

12. Ambao wanatangatanga ovyo katika ujinga wao.

يَسْـَٔلُوْنَ اَيَّانَ يَوْمُ الدِّيْنِ ⑬

13. Wanauliza ni lini Siku ya Hukumu?

يَوْمَ هُمْ عَلَى النَّارِ يُفْتَنُوْنَ ⑭

14. Siku watakayochomwa Motoni.

Sura hii imepata jina lake katika neno la kwanza la Aya ya 2. Sura hii ilishuka Makka.

15. Onjeni matokeo ya udanganyifu wenu. Haya ndiyo mliyokuwa mkiyaharakia.

ذُوْقُوْا فِتْنَتَكُمْ ؕ هٰذَا الَّذِیْ كُنْتُمْ بِهٖ تَسْتَعْجِلُوْنَ ﴿۱۵﴾

16. Kwa yakini wamchao Allah watakuwa katika Mabustani na chemchem,

اِنَّ الْمُتَّقِیْنَ فِیْ جَنّٰتٍ وَّ عُیُوْنٍ ﴿۱۶﴾

17. Wakipokea aliyowapa Mola wao. Kwa hakika wao walikuwa wakifanya wema kabla ya haya:

اٰخِذِیْنَ مَاۤ اٰتٰىهُمْ رَبُّهُمْ ؕ اِنَّهُمْ كَانُوْا قَبْلَ ذٰلِكَ مُحْسِنِیْنَ ﴿۱۷﴾ؕ

18. Walikuwa wakilala kidogo tu usiku,

كَانُوْا قَلِیْلًا مِّنَ الَّیْلِ مَا یَهْجَعُوْنَ ﴿۱۸﴾

19. Na wanaomba msamaha nyakati za kabla ya alfajiri.

وَ بِالْاَسْحَارِ هُمْ یَسْتَغْفِرُوْنَ ﴿۱۹﴾

20. Na katika mali zao imo hisa ya aombaye na ajizuiaye (kuomba).

وَ فِیْۤ اَمْوَالِهِمْ حَقٌّ لِّلسَّآىِٕلِ وَ الْمَحْرُوْمِ ﴿۲۰﴾

21. Na katika ardhi zimo Ishara kwa wenye yakini;

وَ فِی الْاَرْضِ اٰیٰتٌ لِّلْمُوْقِنِیْنَ ﴿۲۱﴾ۙ

22. Na katika nafsi zenu; je, hamwoni?

وَ فِیْۤ اَنْفُسِكُمْ ؕ اَفَلَا تُبْصِرُوْنَ ﴿۲۲﴾

23. Na katika mbingu ziko riziki zenu na mliyoahidiwa.

وَ فِی السَّمَآءِ رِزْقُكُمْ وَ مَا تُوْعَدُوْنَ ﴿۲۳﴾

24. Basi kwa kiapo cha Mola wa mbingu na ardhi kwa hakika hayo ni haki kama ilivyo (haki) ya kwamba ninyi mnasema.

فَوَ رَبِّ السَّمَآءِ وَ الْاَرْضِ اِنَّهٗ لَحَقٌّ مِّثْلَ مَاۤ اَنَّكُمْ تَنْطِقُوْنَ ﴿۲۴﴾ع ۱۸

FUNGU 2

25. Je, imekufikia hadithi ya wageni waheshimiwao wa Ibrahimu?

هَلْ اَتٰىكَ حَدِیْثُ ضَیْفِ اِبْرٰهِیْمَ الْمُكْرَمِیْنَ ﴿۲۵﴾ۘ وقف لازم

Aya 20. *Mahruum,* "Ajizuiaye," yaani maskini asiyeoomba (Kashshaf). Pia maana yake ni asiye na kipawa cha kusema, kama wanyama (Lane). Wenye mali wajue ya kuwa katika mali zao iko haki maalumu kwa ajili ya masikini na mafukara na wanyama. Wasifikiri kuwa mali hizo ni zao peke yao. Kama fundisho hili lingeshikwa kwa uaminifu, na maskini na wahitaji wakapewa haki zao, mali zingetumika vyema na machafuko mengi yangekwisha duniani na mengine yasingetokea.

Aya 25-28. Katika Aya hizi zimeelezwa habari sita zinazotakiwa kushikwa kwa ajili ya wageni: (1) kuwalaki kwa uso mcheshi na kwa moyo uliokunjuka; (2) kuonyesha furaha kwa ulimi na kuwaamkia kwa maamkio ya salaam ambayo ni kuwaombea dua ya salama; (3) kuwaletea

26. Walipoingia kwake wakasema: Salaam. Akasema: Salaam, (na akasema moyoni; hawa wanaonekana kuwa ni) watu wageni;

اِذْ دَخَلُوْا عَلَيْهِ فَقَالُوْا سَلٰمًا ؕ قَالَ سَلٰمٌ ۚ قَوْمٌ مُّنْكَرُوْنَ ﴿۲۵﴾

27. Mara akaenda kwa ahali zake na akaleta ndama mnono (aliyekaangwa),

فَرَاغَ اِلٰٓى اَهْلِهٖ فَجَآءَ بِعِجْلٍ سَمِيْنٍ ﴿۲۶﴾

28. Na akamuweka mbele yao. Akauliza: Je, hamtokula?

فَقَرَّبَهٗٓ اِلَيْهِمْ قَالَ اَلَا تَاْكُلُوْنَ ﴿۲۷﴾

29. Basi akawaonea hofu. Wakasema: Usiogope, na wakamtolea habari nzuri za mtoto mwenye elimu.

فَاَوْجَسَ مِنْهُمْ خِيْفَةً ؕ قَالُوْا لَا تَخَفْ ؕ وَبَشَّرُوْهُ بِغُلٰمٍ عَلِيْمٍ ﴿۲۸﴾

30. Ndipo mkewe akawaelekea akipaza sauti na akajipiga usoni na kusema: (Mimi) mwanamke mzee, tasa!

فَاَقْبَلَتِ امْرَاَتُهٗ فِىْ صَرَّةٍ فَصَكَّتْ وَجْهَهَا وَقَالَتْ عَجُوْزٌ عَقِيْمٌ ﴿۲۹﴾

31. Wakasema: Ndivyo hivyo, Amesema Mola wako; hakika Yeye ndiye Mwenye hekima Ajuaye.

قَالُوْا كَذٰلِكِ ۙ قَالَ رَبُّكِ ؕ اِنَّهٗ هُوَ الْحَكِيْمُ الْعَلِيْمُ ﴿۳۰﴾

JUZU 27

32. Akasema: basi makusudio yenu ni nini, Enyi mliotumwa?

قَالَ فَمَا خَطْبُكُمْ اَيُّهَا الْمُرْسَلُوْنَ ﴿۳۱﴾

33. Wakasema: Hakika sisi tumetumwa kwa watu wakosefu,

قَالُوْٓا اِنَّآ اُرْسِلْنَآ اِلٰى قَوْمٍ مُّجْرِمِيْنَ ﴿۳۲﴾

34. Ili tuwatupie juu yao mawe ya udongo.

لِنُرْسِلَ عَلَيْهِمْ حِجَارَةً مِّنْ طِيْنٍ ﴿۳۳﴾

35. Yaliyowekwa alama, kwa ajili ya watu wapitao kiasi kwa Mola wako.

مُّسَوَّمَةً عِنْدَ رَبِّكَ لِلْمُسْرِفِيْنَ ﴿۳۴﴾

36. Kwa hiyo Tukawatoa waaminio waliokuwa humo.

فَاَخْرَجْنَا مَنْ كَانَ فِيْهَا مِنَ الْمُؤْمِنِيْنَ ﴿۳۵﴾

37. Lakini Hatukupata humo ila nyumba moja tu ya wale waliosilimu.

فَمَا وَجَدْنَا فِيْهَا غَيْرَ بَيْتٍ مِّنَ الْمُسْلِمِيْنَ ﴿۳۶﴾

---

chakula bila wao kuomba wala wenyeji kuwauliza kama wanakitaka; (4) kuwapa chakula kilicho kizuri na kinachopatikana nyumbani bila taabu; (5) mwenye nyumba mwenyewe alete chakula kuwaandalia; (6) kuwakalisha pahali wanapoweza kula bila taabu na kwa raha.

Aya 33. *Wakosefu,* yaani watu wa Nabii Luti.

Aya 35. *Musrifiin,* "Wapitao kiasi" ni watu wenye dhambi ambao wanavunja kanuni zilizowekwa na Sheria.

وَتَرَكْنَا فِيهَآ اٰيَةً لِّلَّذِيْنَ يَخَافُوْنَ الْعَذَابَ الْاَلِيْمَ ﴿٣٨﴾

38. Na Tukaacha humo Ishara kwa ajili ya wale wanaoogopa adhabu iumizayo.

وَفِيْ مُوْسٰٓى اِذْ اَرْسَلْنٰهُ اِلٰى فِرْعَوْنَ بِسُلْطٰنٍ مُّبِيْنٍ ﴿٣٩﴾

39. Na katika (habari za) Musa (ilikuwepo pia Ishara ya aina hii), Tulipomtuma kwa Firauni na dalili waziwazi.

فَتَوَلّٰى بِرُكْنِهٖ وَقَالَ سٰحِرٌ اَوْ مَجْنُوْنٌ ﴿٤٠﴾

40. Akakengeuka pamoja na wajumbe wake na akasema: Huyu ni mchawi au majnuni.

فَاَخَذْنٰهُ وَجُنُوْدَهٗ فَنَبَذْنٰهُمْ فِي الْيَمِّ وَهُوَ مُلِيْمٌ ﴿٤١﴾

41. Basi Tukamkamata yeye na majeshi yake na Tukawatupa baharini, na yeye alikuwa mlaumiwa.

وَفِيْ عَادٍ اِذْ اَرْسَلْنَا عَلَيْهِمُ الرِّيْحَ الْعَقِيْمَ ﴿٤٢﴾

42. Na kwa Waadi pia (kulikuwepo na Ishara), Tulipowapelekea upepo uangamizao.

مَا تَذَرُ مِنْ شَيْءٍ اَتَتْ عَلَيْهِ اِلَّا جَعَلَتْهُ كَالرَّمِيْمِ ﴿٤٣﴾

43. Haukuacha cho chote ulichokifikia ila ulikifanya kama kitu kilichooza.

وَفِيْ ثَمُوْدَ اِذْ قِيْلَ لَهُمْ تَمَتَّعُوْا حَتّٰى حِيْنٍ ﴿٤٤﴾

44. Na kwa Wathamudi pia (kulikuwepo na Ishara), walipoambiwa: Jinufaisheni kwa muda kidogo.

فَعَتَوْا عَنْ اَمْرِ رَبِّهِمْ فَاَخَذَتْهُمُ الصّٰعِقَةُ وَهُمْ يَنْظُرُوْنَ ﴿٤٥﴾

45. Lakini wakaasi amri ya Mola wao, mara rindimo likawakamata hali wanatazama.

فَمَا اسْتَطَاعُوْا مِنْ قِيَامٍ وَّمَا كَانُوْا مُنْتَصِرِيْنَ ﴿٤٦﴾

46. Basi hawakuweza kusimama wala hawakuwa wenye uwezo wa kujilipiza.

وَقَوْمَ نُوْحٍ مِّنْ قَبْلُ ۭ اِنَّهُمْ كَانُوْا قَوْمًا فٰسِقِيْنَ ﴿٤٧﴾

47. Na watu wa Nuhu pia (waliokuwa) kabla (ya hawa), hakika wao walikuwa watu waasi.

FUNGU 3

وَالسَّمَاۗءَ بَنَيْنٰهَا بِاَيْىدٍ وَّاِنَّا لَمُوْسِعُوْنَ ﴿٤٨﴾

48. Na Tumeijenga mbingu kwa uimara na Tunaendelea kuipanua sana.

وَالْاَرْضَ فَرَشْنٰهَا فَنِعْمَ الْمٰهِدُوْنَ ﴿٤٩﴾

49. Na ardhi Tumeitandaza, basi Watandazaji Wazuri walioje Sisi!

Aya 40. *Biruknihii,* "Kwa sababu ya nguvu zake," pia yanaweza kuwa na maana ya "Pamoja na jamaa zake" yaani Firauni pamoja na watu wake wote walikataa haki.

Aya 44. *Muda kidogo.* Walipewa muda wa siku tatu (sura 11:66).

Aya 48. *Bi aidin,* "Kwa kudra." Neno *aidin* maana yake ni mikono, uwezo, nguvu na kudra.

50. Na katika kila kitu Tumeumba jozi ili mpate kushika nasaha.

وَمِنْ كُلِّ شَيْءٍ خَلَقْنَا زَوْجَيْنِ لَعَلَّكُمْ تَذَكَّرُوْنَ ﴿٥٠﴾

51. Basi kimbilieni kwa Allah, mimi kwenu ni Mwonyaji waziwazi kutoka Kwake.

فَفِرُّوْٓا اِلَى اللّٰهِ ؕ اِنِّيْ لَكُمْ مِّنْهُ نَذِيْرٌ مُّبِيْنٌ ﴿٥١﴾

52. Wala msimfanye mwingine kuwa aabudiwaye pamoja na Allah, bila shaka mimi ni Mwonyaji dhahiri kwenu kutoka Kwake.

وَلَا تَجْعَلُوْا مَعَ اللّٰهِ اِلٰهًا اٰخَرَ ؕ اِنِّيْ لَكُمْ مِّنْهُ نَذِيْرٌ مُّبِيْنٌ ﴿٥٢﴾

53. Hivyo ndivyo hakuna Mtume ye yote aliyewafikia wale wa kabla yao ila walisema: Huyu ni mchawi au majnuni.

كَذٰلِكَ مَآ اَتَى الَّذِيْنَ مِنْ قَبْلِهِمْ مِّنْ رَّسُوْلٍ اِلَّا قَالُوْا سَاحِرٌ اَوْ مَجْنُوْنٌ ﴿٥٣﴾

54. Je, wameusiana kwa jambo hili? Bali hawa ni watu wahalifu.

اَتَوَاصَوْا بِهٖ ۚ بَلْ هُمْ قَوْمٌ طَاغُوْنَ ﴿٥٤﴾

55. Basi waachilie mbali, nawe si mwenye kulaumiwa.

فَتَوَلَّ عَنْهُمْ فَمَآ اَنْتَ بِمَلُوْمٍ ﴿٥٥﴾

56. Na endelea kukumbusha; kwa yakini ukumbusho huwafaa waaminio.

وَّذَكِّرْ فَاِنَّ الذِّكْرٰى تَنْفَعُ الْمُؤْمِنِيْنَ ﴿٥٦﴾

57. Sikuwaumba majinni na watu ila wapate kuniabudu.

وَمَا خَلَقْتُ الْجِنَّ وَالْاِنْسَ اِلَّا لِيَعْبُدُوْنِ ﴿٥٧﴾

58. Sitaki riziki kutoka kwao wala Sitaki wanilishe.

مَآ اُرِيْدُ مِنْهُمْ مِّنْ رِّزْقٍ وَّمَآ اُرِيْدُ اَنْ يُّطْعِمُوْنِ ﴿٥٨﴾

59. Kwa yakini Allah ndiye Mtoaji wa riziki, Mwenye nguvu, Mwenye sifa madhubuti.

اِنَّ اللّٰهَ هُوَ الرَّزَّاقُ ذُو الْقُوَّةِ الْمَتِيْنُ ﴿٥٩﴾

60. Hakika kwa wale waliodhulumu itakuwa sehemu kama sehemu ya watu wa jinsi yao, hivyo wasinihimize.

فَاِنَّ لِلَّذِيْنَ ظَلَمُوْا ذَنُوْبًا مِّثْلَ ذَنُوْبِ اَصْحٰبِهِمْ فَلَا يَسْتَعْجِلُوْنِ ﴿٦٠﴾

61. Basi ole kwa wale walioikataa siku yao wanayoahidiwa.

فَوَيْلٌ لِّلَّذِيْنَ كَفَرُوْا مِنْ يَّوْمِهِمُ الَّذِيْ يُوْعَدُوْنَ ﴿٦١﴾ ع ٢

Aya 50. Zamani Waarabu walikuwa wanajua kuwa katika mitende kuna jike na dume. Na Kurani ilieleza ya kuwa bali ni kila kitu chenye "jike na dume," na uchunguzi wa siku hizi wa elimu za maarifa umehakikisha ya kwamba katika kila kitu, mawe, umeme, na vinginevyo kuna "jike na dume."

Aya 51. Kama mama anampiga mtoto, mtoto hukimbilia kwa yeye huyo mama yake. Basi kama mtu anapata taabu asikimbilie kwingine bali kwa Allah.

Aya 57. *Ila wapate kuniabudu,* pia maana yake, *ila wapate kunifahamu* (Bukhari). Kusudi la kweli la maisha ya binadamu ni kumjua Mungu kama ipasavyo na kumwabudu na kujitia kabisa katika mapenzi Yake hata kila alitendalo au alisemalo mtu liwe kwa ajili ya Mungu tu (Uislamu na Hekima yake).

سُوْرَةُ الطُّوْرِ مَكِّيَّةٌ وَّ هِيَ مَعَ الْبَسْمَلَةِ خَمْسُوْنَ اٰيَةً وَّ رُكُوْعَانِ

52. SURA AT-TUUR

Imeteremshwa Makka

Ina mafungu 2 na Aya 50 pamoja na Bismillahi

بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ ①

1. Kwa jina la Allah, Mwingi wa rehema, Mwingi wa ukarimu.

وَالطُّوْرِ ۙ ②

2. Naapa kwa Tuur (Mlima),

وَكِتٰبٍ مَّسْطُوْرٍ ۙ ③

3. Na kwa Kitabu kilichoandikwa.

فِيْ رَقٍّ مَّنْشُوْرٍ ۙ ④

4. Katika waraka wa ngozi uliofunuliwa,

وَّالْبَيْتِ الْمَعْمُوْرِ ۙ ⑤

5. Na kwa nyumba inayozuriwa,

وَالسَّقْفِ الْمَرْفُوْعِ ۙ ⑥

6. Na kwa paa lililonyanyuliwa,

وَالْبَحْرِ الْمَسْجُوْرِ ۙ ⑦

7. Na kwa bahari yenye tufani.

اِنَّ عَذَابَ رَبِّكَ لَوَاقِعٌ ۙ ⑧

8. Kwa yakini adhabu ya Mola wako itatokea.

مَّا لَهٗ مِنْ دَافِعٍ ۙ ⑨

9. Hakuna atakayeizuia.

يَّوْمَ تَمُوْرُ السَّمَآءُ مَوْرًا ۙ ⑩

10. Siku itakapotikisika mbingu kwa mtikisiko.

وَّتَسِيْرُ الْجِبَالُ سَيْرًا ؕ ⑪

11. Na milima itasogea msogeo mkubwa.

فَوَيْلٌ يَّوْمَئِذٍ لِّلْمُكَذِّبِيْنَ ۙ ⑫

12. Basi ole siku hiyo kwa wakadhibishao,

Sura hii inaitwa *Mlima* kwa sababu Allah anaapa kwa mlima katika Aya ya 2. Mlima huo ni kule alikoitwa Nabii Musa na Allah, hivyo inaonyesha kufanana kulioko baina ya Mtume *s.a.w.* na Nabii Musa, maana Mtume *s.a.w* pia alipokea wahyi katika pango la mlima.

Aya 2. Neno *Tuur* ni "mlima" na hapa linahusu mlima Turi ulioko Sinai, alikokwenda Nabii Musa kupokea Sheria aliyofunuliwa na Allah.

Aya 4. *Raqqin,* "waraka wa ngozi" ni ngozi nyembamba, nyeupe ya mnyama iliyotengenezwa kama karatasi ya kuandikia.

الَّذِيْنَ هُمْ فِيْ خَوْضٍ يَّلْعَبُوْنَ ﴿١٣﴾

13. Ambao wanacheza katika mambo ya upuuzi.

يَوْمَ يُدَعُّوْنَ اِلٰى نَارِ جَهَنَّمَ دَعًّا ﴿١٤﴾

14. Siku watakaposukumwa kwenye moto wa Jahanamu msukumo wa nguvu.

هٰذِهِ النَّارُ الَّتِيْ كُنْتُمْ بِهَا تُكَذِّبُوْنَ ﴿١٥﴾

15. Huu ndio Moto ambao mlikuwa mkiukadhibisha.

اَفَسِحْرٌ هٰذَآ اَمْ اَنْتُمْ لَا تُبْصِرُوْنَ ﴿١٦﴾

16. Basi, je! huu ni uchawi au mlikuwa hamtumii busara?

اِصْلَوْهَا فَاصْبِرُوْٓا اَوْ لَا تَصْبِرُوْا ۚ سَوَآءٌ عَلَيْكُمْ ؕ اِنَّمَا تُجْزَوْنَ مَا كُنْتُمْ تَعْمَلُوْنَ ﴿١٧﴾

17. Uingieni, mkingoja au msingoje ni mamoja kwenu; mtalipwa tu mliyokuwa mkiyatenda.

اِنَّ الْمُتَّقِيْنَ فِيْ جَنّٰتٍ وَّ نَعِيْمٍ ﴿١٨﴾

18. Kwa yakini wamchao (Allah) watakuwa katika Pepo na neema,

فٰكِهِيْنَ بِمَآ اٰتٰىهُمْ رَبُّهُمْ ۚ وَ وَقٰىهُمْ رَبُّهُمْ عَذَابَ الْجَحِيْمِ ﴿١٩﴾

19. Wakifurahia yale Aliyowapa Mola wao, na Mola wao Atawalinda na adhabu ya Jahannam.

كُلُوْا وَاشْرَبُوْا هَنِيْٓـًٔا بِمَا كُنْتُمْ تَعْمَلُوْنَ ﴿٢٠﴾

20. (Wataambiwa) kuleni na kunyweni kwa faraja kwa sababu ya hayo mliyokuwa mkiyatenda.

مُتَّكِـِٕيْنَ عَلٰى سُرُرٍ مَّصْفُوْفَةٍ ۚ وَزَوَّجْنٰهُمْ بِحُوْرٍ عِيْنٍ ﴿٢١﴾

21. Wakiegemea juu ya viti vya fahari vilivyopangwa safu safu, na Tutawapa wenzi wa kike walio mabikira wenye macho ya vikombe.

Aya 21. *Tutawapa wenzi wa kike walio mabikira wenye macho ya vikombe.* Wanawake watakatifu ni neema mojawapo katika neema za Peponi. Mapadre wanasema ya kuwa Mtume *s.a.w.* aliwabembeleza watu kuingia katika dini yake kwa kuwataja wanawake kuwa malipo ya waaminio. Majibu yake ni haya:-

1. Maisha ya masahaba wa Mtume *s.a.w.* waliodharauliwa na kuteswa mateso ya kila aina kwa ajili ya dini yaubatilisha upinzani huu mara moja. Walikuwa wamekubali kuchinjwa kama mbuzi na kondoo kwa kupata radhi ya Mola. Wake kwa waume wakaonyesha subira na unyenyekevu usiopatikana mfano wake katika umati wa Nabii awaye yote. Kuwasingizia tamaa watu watawa kama hao ni dhuluma kubwa.

2. Kurani haioni mwanamke kuwa ni shina la dhambi na mwenye kumkosesha mumewe. Kwa hakika mwanamke mcha-Mungu humwongezea mwenzake raha na utulivu wa moyo (sura 30:22).

3. Yesu Kristo aliwaambia wanafunzi wake akisema, "Hapana mtu aliyeacha nyumba, au ndugu wa kiume au ndugu wa kike, au baba, au mama, au mke, au watoto au mashamba kwa ajili yangu, au kwa ajili ya Injili, ila atapewa mara mia saba wakati huu" (Marko 10:29-30; Luka 18:29-30; Mattayo 19:29). Mtu kupewa mke mara mia ni tamaa kubwa mno, tena ni jambo la kimwili hasa. Lakini walidanganywa bure. Hata mmoja miongoni mwao hakupokea hivyo walivyoahidiwa na Yesu. Na kupata wazazi zaidi mara nyingi ni msiba. Je, hizo ndizo zawadi ambazo Wakristo wanafurahia?

وَالَّذِيْنَ اٰمَنُوْا وَاتَّبَعَتْهُمْ ذُرِّيَّتُهُمْ بِاِيْمَانٍ اَلْحَقْنَا بِهِمْ ذُرِّيَّتَهُمْ وَمَآ اَلَتْنٰهُمْ مِّنْ عَمَلِهِمْ مِّنْ شَيْءٍ ؕ كُلُّ امْرِئٍۢ بِمَا كَسَبَ رَهِيْنٌ ﴿٢١﴾

22. Na wale walioamini na wazao wao wakawafuata katika imani, Tutawaunga kwao wazao wao, wala Hatutawapunja kitu katika vitendo vyao, kila mtu ni rehani wa alichokichuma.

وَاَمْدَدْنٰهُمْ بِفَاكِهَةٍ وَّلَحْمٍ مِّمَّا يَشْتَهُوْنَ ﴿٢٢﴾

23. Na Tutawasaidia kwa matunda na nyama katika vile watakavyopenda.

يَتَنَازَعُوْنَ فِيْهَا كَاْسًا لَّا لَغْوٌ فِيْهَا وَلَا تَاْثِيْمٌ ﴿٢٣﴾

24. Watapeana humo bakuli (lenye kinywaji) kisicholeta upuuzi wala dhambi.

وَيَطُوْفُ عَلَيْهِمْ غِلْمَانٌ لَّهُمْ كَاَنَّهُمْ لُؤْلُؤٌ مَّكْنُوْنٌ ﴿٢٤﴾

25. Na wavulana wao watawazungukazunguka kana kwamba ni lulu zilizofichwa.

وَاَقْبَلَ بَعْضُهُمْ عَلٰى بَعْضٍ يَّتَسَآءَلُوْنَ ﴿٢٥﴾

26. Na wataelekeana wao kwa wao wakiulizana,

قَالُوْٓا اِنَّا كُنَّا قَبْلُ فِيْٓ اَهْلِنَا مُشْفِقِيْنَ ﴿٢٦﴾

27. Watasema: Bila shaka tulikuwa zamani katika ahali zetu tukiogopa.

فَمَنَّ اللّٰهُ عَلَيْنَا وَوَقٰىنَا عَذَابَ السَّمُوْمِ ﴿٢٧﴾

28. Lakini Allah Ametufanyia ihsani na Ametuokoa na adhabu ya upepo wa Moto.

اِنَّا كُنَّا مِنْ قَبْلُ نَدْعُوْهُ ؕ اِنَّهٗ هُوَ الْبَرُّ الرَّحِيْمُ ﴿٢٨﴾ ع ١ ٣

29. Hakika sisi zamani tulikuwa tukimwomba Yeye: hakika Yeye ndiye Mwema, Mwenye rehema.

FUNGU 2

فَذَكِّرْ فَمَآ اَنْتَ بِنِعْمَتِ رَبِّكَ بِكَاهِنٍ وَّلَا مَجْنُوْنٍ ؕ ﴿٢٩﴾

30. Basi ukumbushe, na wewe kwa neema za Mola wako si kahini wala majnuni.

Kurani inawatangazia waaminio habari njema ya kuwaweka Peponi pamoja na kizazi chao wakiamini na kutenda mema (sura 52:22).

4. Wakati Yesu alipoulizwa habari ya ulimwengu ujao alijibu akasema, "kwa maana katika kiyama hawaoi wala hawaolewi" (Matt. 22:30). Lakini aliposema habari ya kuja kwake mara ya pili, ambayo ni baada ya kufufuka katika wafu kama wanavyokiri Wakristo, alijifananisha na bwana arusi ajaye usiku wa manane na kuingia arusini pamoja na wanawali watano wenye busara na kufunga mlango (Matt. 25:1-10).

Aya 22. *Kila mtu ni rehani ya alichokichuma,* yaani mtu mwingine hatakuwa na madaraka ya uchumi wa mtu mwingine; ukiwa ni uchumi mwema au mbaya, ni juu ya yule yule aliyeuchuma.

Aya 30. *Kwa neema za Mola wako,* yaani neema za Mwenyezi Mungu unazopewa zitahakikisha kuwa wewe si mganga wala mwehu.

31. Au wanasema: (Huyu) mshairi tunamtazamia kupatwa na mashaka ya dahari.

اَمْ يَقُوْلُوْنَ شَاعِرٌ نَّتَرَبَّصُ بِهٖ رَيْبَ الْمَنُوْنِ ﴿٣١﴾

32. Sema: Ngojeni na mimi pia ni pamoja nanyi katika wangojeao.

قُلْ تَرَبَّصُوْا فَاِنِّيْ مَعَكُمْ مِّنَ الْمُتَرَبِّصِيْنَ ﴿٣٢﴾

33. Je! Akili zao zinawaamuru haya au wao ni watu waasi?

اَمْ تَاْمُرُهُمْ اَحْلَامُهُمْ بِهٰذَآ اَمْ هُمْ قَوْمٌ طَاغُوْنَ ﴿٣٣﴾

34. Au wanasema: (Kurani) ameitunga yeye mwenyewe? Bali wao hawaamini.

اَمْ يَقُوْلُوْنَ تَقَوَّلَهٗ ۚ بَلْ لَّا يُؤْمِنُوْنَ ﴿٣٤﴾

35. Basi walete hadithi kama hii ikiwa wanasema kweli.

فَلْيَاْتُوْا بِحَدِيْثٍ مِّثْلِهٖٓ اِنْ كَانُوْا صٰدِقِيْنَ ﴿٣٥﴾

36. Je, wameumbwa pasipo kitu, au wao ndio waumbaji?

اَمْ خُلِقُوْا مِنْ غَيْرِ شَيْءٍ اَمْ هُمُ الْخٰلِقُوْنَ ﴿٣٦﴾

37. Au wameumba mbingu na ardhi? Bali hawana yakini.

اَمْ خَلَقُوا السَّمٰوٰتِ وَالْاَرْضَ ۚ بَلْ لَّا يُوْقِنُوْنَ ﴿٣٧﴾

38. Au wanazo hazina za Mola wako au wao ndio walinzi?

اَمْ عِنْدَهُمْ خَزَآئِنُ رَبِّكَ اَمْ هُمُ الْمُصَيْطِرُوْنَ ﴿٣٨﴾

39. Au wanayo ngazi ya (kupandia na) kusikilizia? Basi msikiaji wao alete dalili iliyo wazi.

اَمْ لَهُمْ سُلَّمٌ يَّسْتَمِعُوْنَ فِيْهِ ۚ فَلْيَاْتِ مُسْتَمِعُهُمْ بِسُلْطٰنٍ مُّبِيْنٍ ﴿٣٩﴾

40. Au Yeye Anao mabinti nanyi mnao watoto wa kiume?

اَمْ لَهُ الْبَنٰتُ وَلَكُمُ الْبَنُوْنَ ﴿٤٠﴾

41. Au unawaomba ujira kwa hiyo wanalemewa na gharama?

اَمْ تَسْـَٔلُهُمْ اَجْرًا فَهُمْ مِّنْ مَّغْرَمٍ مُّثْقَلُوْنَ ﴿٤١﴾

42. Au iko kwao (elimu ya) ghaibu nao wanaandika.

اَمْ عِنْدَهُمُ الْغَيْبُ فَهُمْ يَكْتُبُوْنَ ﴿٤٢﴾

Aya 35. *Basi walete hadithi kama hii.* Ndiyo mashindano wanayopewa makafiri na daima wameshindwa. Wanaambiwa, kama Mtume *s.a.w.* ni mwehu au mganga au ameyatunga mwenyewe meneno haya basi walete maneno ya namna hii toka kwa mganga au mwehu au mtungaji mwingine ikiwa wanasema kweli.

43. Au wanaitaka hila? Lakini waliokufuru ndio watakaotegwa na hila.

اَمْ يُرِيْدُوْنَ كَيْدًا ؕ فَالَّذِيْنَ كَفَرُوْا هُمُ الْمَكِيْدُوْنَ ﴿٤٢﴾

44. Au yuko kwao anayeabudiwa ghairi ya Allah? Allah Ametakasika na hao wanaomshirikisha naye.

اَمْ لَهُمْ اِلٰهٌ غَيْرُ اللّٰهِ ؕ سُبْحٰنَ اللّٰهِ عَمَّا يُشْرِكُوْنَ ﴿٤٣﴾

45. Na kama wakiona kipande cha mbingu kikianguka husema: Ni mawingu yanayobebana.

وَاِنْ يَّرَوْا كِسْفًا مِّنَ السَّمَآءِ سَاقِطًا يَّقُوْلُوْا سَحَابٌ مَّرْكُوْمٌ ﴿٤٤﴾

46. Basi waachie mpaka wakutane na siku watakayoangushiwa umeme!

فَذَرْهُمْ حَتّٰى يُلٰقُوْا يَوْمَهُمُ الَّذِىْ فِيْهِ يُصْعَقُوْنَ ﴿٤٥﴾

47. Siku ambayo hila zao hazitawafaa hata kidogo wala hawatasaidiwa.

يَوْمَ لَا يُغْنِىْ عَنْهُمْ كَيْدُهُمْ شَيْـًٔا وَّلَا هُمْ يُنْصَرُوْنَ ﴿٤٦﴾

48. Na kwa yakini wale waliodhulumu watakuwa na adhabu zaidi ya hiyo, lakini wengi wao hawajui.

وَاِنَّ لِلَّذِيْنَ ظَلَمُوْا عَذَابًا دُوْنَ ذٰلِكَ وَلٰكِنَّ اَكْثَرَهُمْ لَا يَعْلَمُوْنَ ﴿٤٧﴾

49. Na usubiri kwa ajili ya amri ya Mola wako, na hakika wewe uko mbele ya macho Yetu; na Mtukuze kwa kumsifu Mola wako unaposimama.

وَاصْبِرْ لِحُكْمِ رَبِّكَ فَاِنَّكَ بِاَعْيُنِنَا وَسَبِّحْ بِحَمْدِ رَبِّكَ حِيْنَ تَقُوْمُ ﴿٤٨﴾

50. Na katika usiku pia Mtukuze na zichwapo nyota.

وَمِنَ الَّيْلِ فَسَبِّحْهُ وَاِدْبَارَ النُّجُوْمِ ﴿٤٩﴾ ع ٢

سُوْرَةُ النَّجْمِ مَكِّيَّةٌ وَّ هِيَ مَعَ الْبَسْمَلَةِ ثَلَا ثٌ وَّ سِتُّوْنَ اٰيَةً وَّ ثَلَا ثَةُ رُكُوْعَاتٍ

53. SURA AN-NAJM

Imeteremshwa Makka

Ina mafungu 3 na Aya 63 pamoja na Bismillahi

بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ ①

1. Kwa jina la Allah, Mwingi wa rehema, Mwingi wa ukarimu.

وَالنَّجْمِ اِذَا هَوٰى ۙ②

2. Naapa kwa nyota itakapoanguka,

مَا ضَلَّ صَاحِبُكُمْ وَمَا غَوٰى ۚ③

3. Sahibu yenu hakupotea wala hakukosa,

وَمَا يَنْطِقُ عَنِ الْهَوٰى ؕ④

4. Wala hasemi kwa tamaa (ya nafsi yake).

اِنْ هُوَ اِلَّا وَحْيٌ يُّوْحٰى ۙ⑤

5. Huo ni ufunuo tu unaofunuliwa.

عَلَّمَهٗ شَدِيْدُ الْقُوٰى ۙ⑥

6. Amemfundisha Aliye ni Mwenye nguvu sana,

ذُوْ مِرَّةٍ ؕ فَاسْتَوٰى ۙ⑦

7. Mwenye Hekima kubwa Hivyo akafanikiwa.

وَهُوَ بِالْاُفُقِ الْاَعْلٰى ؕ⑧

8. Alipokuwa katika upeo wa juu kabisa.

ثُمَّ دَنَا فَتَدَلّٰى ۙ⑨

9. Kisha akakaribia hivyo akateremka.

فَكَانَ قَابَ قَوْسَيْنِ اَوْ اَدْنٰى ۚ⑩

10. Ndipo akawa umbali wa pinde mbili au karibu zaidi.

فَاَوْحٰۤى اِلٰى عَبْدِهٖ مَاۤ اَوْحٰى ؕ⑪

11. Hivyo Akamfunulia Mtumishi Wake Wahyi Alioufunua.

مَا كَذَبَ الْفُؤَادُ مَا رَاٰى ⑫

12. Moyo haukusema uwongo kuhusiana na yale uliyoyaona.

اَفَتُمٰرُوْنَهٗ عَلٰى مَا يَرٰى ⑬

13. Je! mnabishana naye juu ya yale aliyoyaona?

Sura hii inaitwa *Nyota,* na neno hilo liko katika Aya yake ya pili. Sura hii ilishuka Makka katika mwaka wa tano wa Hijra.

Aya 2. Katika nchi ya Bara Arabu kuanguka kwa nyota walitabiri ni kufika kwa mtu mkubwa. Aya hii na zifuatazo zinatoa dalili za kuhakikisha ukweli na adhma na shani na utukufu wa Mtume *s.a.w.*

Kadhalika katika Aya hizi mmelezwa habari za *Mi'iraaj* ya Mtume *s.a.w.;* na habari zinazokuja katika Hadithi na historia zinapatana na maelezo ya *Mi'iraaj* yaliyomo katika Aya hizi.

وَلَقَدْ رَاٰهُ نَزْلَةً اُخْرٰى ﴿١٣﴾

14. Na bila shaka yeye ameshaiona katika hali nyingine pia,

عِنْدَ سِدْرَةِ الْمُنْتَهٰى ﴿١٤﴾

15. Penye mkunazi uliopo kwenye upeo wa mwisho kabisa;

عِنْدَهَا جَنَّةُ الْمَاْوٰى ﴿١٥﴾

16. Karibu yake pana Bustani inayohifadhi.

اِذْ يَغْشَى السِّدْرَةَ مَا يَغْشٰى ﴿١٦﴾

17. Kilipofunika mkunazi kilichofunika.

مَا زَاغَ الْبَصَرُ وَمَا طَغٰى ﴿١٧﴾

18. Jicho halikuhangaika wala halikuruka mpaka.

لَقَدْ رَاٰى مِنْ اٰيٰتِ رَبِّهِ الْكُبْرٰى ﴿١٨﴾

19. Kwa yakini ameona ishara kubwa kabisa kati ya ishara za Mola Wake.

اَفَرَءَيْتُمُ اللّٰتَ وَالْعُزّٰى ﴿١٩﴾

20. Je! Mmewaona Lat na Uzza,

وَمَنٰوةَ الثَّالِثَةَ الْاُخْرٰى ﴿٢٠﴾

21. Na Manat, mwingine wa tatu?

اَلَكُمُ الذَّكَرُ وَلَهُ الْاُنْثٰى ﴿٢١﴾

22. Je! kwenu wa kiume na Kwake wa kike?

تِلْكَ اِذًا قِسْمَةٌ ضِيْزٰى ﴿٢٢﴾

23. Huo tena ni mgawanyo mbaya sana!

اِنْ هِىَ اِلَّاۤ اَسْمَآءٌ سَمَّيْتُمُوْهَاۤ اَنْتُمْ وَاٰبَآؤُكُمْ مَّاۤ اَنْزَلَ اللّٰهُ بِهَا مِنْ سُلْطٰنٍ ؕ اِنْ يَّتَّبِعُوْنَ اِلَّا الظَّنَّ وَمَا تَهْوَى الْاَنْفُسُ ۚ وَلَقَدْ جَآءَهُمْ مِّنْ رَّبِّهِمُ الْهُدٰى ﴿٢٣﴾

24. Siyo haya ila ni majina mliyowapa ninyi na baba zenu: Allah Hakuteremsha dalili juu yao. Hawafuati ila dhana na zinayoyapenda nafsi (zao); na kwa yakini mwongozo umewafikia kutoka kwa Mola wao.

Aya 20-22. *Laat* na *'Uzza* na *Manaat* walikuwa masanamu waliokuwa wanaabudiwa na makafiri wa Makka. Na katika Aya hizi waungu hawa wa uwongo wanasemwa kuwa je, wamepata kuwaonyesha wafuasi wao mambo ambayo Mtume *s.a.w.* ameonyeshwa na Allah?

Mapadre kwa kuangukia juu ya hadithi za uwongo zilizobuniwa na Wakidi wameanza kueleza ya kuwa Mtume kwa kutaka kuwavuta makafiri alikiri kuwa miungu hiyo ya uwongo pia inafaa kuheshimiwa! Jambo kama hili lisingewezekana kabisa kwa Mtume *s.a.w.* na wala hakuna ushahidi wa nje wala wa ndani unaolithibitisha.

Huyo Wakidi ambaye Wakristo wamechukua kwake kisa hiki cha uwongo, wanachuoni wote wakubwa-wakubwa wamemkataa kuwa maneno yake hayategemewi na wametoa ushahidi ulio safi kabisa. Katika Kitabu kiitwacho *Miizaan al-I'tidaal* kinachoeleza habari za maisha ya watu waliosimulia Hadithi za Mtume *s.a.w.* kinasema ya kwamba Wakidi si mtu wa kutegemewa na alikuwa akizua hadithi za uwongo. Mapadre na waandishi wa Kikristo si kama hawajui kuwa Wakidi na wenzake walikuwa watu wanaotunga uwongo; lazima wajue, lakini kwa sababu ya fitina na husuda, wanaziokota hadithi za uwongo na kuziacha makusudi Hadithi sahihi zinazotegemewa na kukubaliwa na Waislamu.

Kisa hiki cha uwongo hakikusimuliwa na Imam Bukhari ambaye ni mtu mashuhuri anayekubaliwa kabisa ukweli wake na ambaye alikuwa katika wakati mmoja na Wakidi.

25. Je mwanadamu apate kila anachotamani?

اَمْ لِلْاِنْسَانِ مَا تَمَنّٰى ﴿٢٥﴾

26. Lakini mwisho na mwanzo ni wa Allah.

فَلِلّٰهِ الْاٰخِرَةُ وَالْاُوْلٰى ﴿٢٦﴾ ع

FUNGU 2

27. Na wako Malaika wangapi mbinguni, ambao uombezi wao hautafaa cho chote isipokuwa baada ya Allah kutoa idhini kwa Amtakaye na kumridhia.

وَكَمْ مِّنْ مَّلَكٍ فِي السَّمٰوٰتِ لَا تُغْنِيْ شَفَاعَتُهُمْ شَيْـًٔا اِلَّا مِنْۢ بَعْدِ اَنْ يَّاْذَنَ اللّٰهُ لِمَنْ يَّشَآءُ وَيَرْضٰى ﴿٢٧﴾

28. Hakika wale wasioiamini Akhera wanawaita Malaika kwa majina ya kike.

اِنَّ الَّذِيْنَ لَا يُؤْمِنُوْنَ بِالْاٰخِرَةِ لَيُسَمُّوْنَ الْمَلٰٓئِكَةَ تَسْمِيَةَ الْاُنْثٰى ﴿٢٨﴾

29. Nao hawana elimu ya haya, hawafuati ila dhana; na kwa hakika dhana haisaidii cho chote mbele ya haki.

وَمَا لَهُمْ بِهٖ مِنْ عِلْمٍ ؕ اِنْ يَّتَّبِعُوْنَ اِلَّا الظَّنَّ ۚ وَاِنَّ الظَّنَّ لَا يُغْنِيْ مِنَ الْحَقِّ شَيْـًٔا ﴿٢٩﴾ ج

30. Basi ujiepushe na yule aupaye kisogo ukumbusho Wetu na wala hataki ila maisha ya dunia.

فَاَعْرِضْ عَنْ مَّنْ تَوَلّٰى ۙ عَنْ ذِكْرِنَا وَلَمْ يُرِدْ اِلَّا الْحَيٰوةَ الدُّنْيَا ﴿٣٠﴾ ط

31. Huo ndiyo upeo wao katika elimu; hakika Mola wako ndiye Amjuaye sana aliyeipotea njia Yake, na Ndiye Amjuaye sana aliyeongoka.

ذٰلِكَ مَبْلَغُهُمْ مِّنَ الْعِلْمِ ؕ اِنَّ رَبَّكَ هُوَ اَعْلَمُ بِمَنْ ضَلَّ عَنْ سَبِيْلِهٖ ۙ وَهُوَ اَعْلَمُ بِمَنِ اهْتَدٰى ﴿٣١﴾ ج

32, Na ni Vya Allah vilivyomo mbinguni na vilivyomo ardhini, ili Awalipe wale waliofanya ubaya kwa yale waliyoyatenda, na ili kuwalipa mema wale waliofanya mema:

وَلِلّٰهِ مَا فِي السَّمٰوٰتِ وَمَا فِي الْاَرْضِ ۙ لِيَجْزِيَ الَّذِيْنَ اَسَآءُوْا بِمَا عَمِلُوْا وَيَجْزِيَ الَّذِيْنَ اَحْسَنُوْا بِالْحُسْنٰى ﴿٣٢﴾ ج

Kadhalika Muhammad bin Is-hak aliyekuwako miaka arubaini kabla ya Wakidi hakusimulia kisa hicho. Hivyo hadithi hiyo ni ya uwongo tu.

Isitoshe Aya ya 24 inasema majina hayo ya *Laat* na *'Uzza* na *Manaat* si cho chote ila ni majina *mliyowapa ninyi na baba zenu; Allah Hakuteremsha dalili juu yao.* Basi baada ya ushahidi huu mashtaka hayo ya Wakristo kuwa Mtume s.a.w. alikubali masanamu yo yote ambayo mtu ameyazoea sana na anaona taabu kuyaacha hayo yaheshimiwe, hayawezi kukubaliwa na mtu ye yote mwenye akili zake.

اَلَّذِيْنَ يَجْتَنِبُوْنَ كَبٰٓئِرَ الْاِثْمِ
وَالْفَوَاحِشَ اِلَّا اللَّمَمَ ؕ اِنَّ رَبَّكَ
وَاسِعُ الْمَغْفِرَةِ ؕ هُوَ اَعْلَمُ بِكُمْ اِذْ
اَنْشَاَكُمْ مِّنَ الْاَرْضِ وَاِذْ اَنْتُمْ اَجِنَّةٌ
فِيْ بُطُوْنِ اُمَّهٰتِكُمْ ۚ فَلَا تُزَكُّوْٓا
اَنْفُسَكُمْ ؕ هُوَ اَعْلَمُ بِمَنِ اتَّقٰى ﴿۳۳﴾ ع

33. Ambao wanajiepusha na madhambi makuu na vitendo vibaya isipokuwa makosa hafifu; bila shaka Mola wako ndiye Mwenye ghofira tele. Yeye ndiye Anayewajueni sana Alipowatoeni katika ardhi na mlipokuwa mimba matumboni mwa mama zenu; basi msijitakase nafsi zenu; Yeye Anamjua sana aliyetakasika.

FUNGU 3

اَفَرَءَيْتَ الَّذِيْ تَوَلّٰى ﴿۳۴﴾

34. Je! Umemwona aliyegeuka?

وَاَعْطٰى قَلِيْلًا وَّاَكْدٰى ﴿۳۵﴾

35. Na akatoa kidogo kisha akajizuia.

اَعِنْدَهٗ عِلْمُ الْغَيْبِ فَهُوَ يَرٰى ﴿۳۶﴾

36. Je! anayo elimu ya yasiyoonekana ambayo kwayo anauona uhakika?

اَمْ لَمْ يُنَبَّاْ بِمَا فِيْ صُحُفِ مُوْسٰى ﴿۳۷﴾

37. Au hakuambiwa yaliyomo katika Vitabu vya Musa?

وَاِبْرٰهِيْمَ الَّذِيْ وَفّٰٓى ﴿۳۸﴾

38. Na vya Ibrahimu aliyetimiza ahadi:

اَلَّا تَزِرُ وَازِرَةٌ وِّزْرَ اُخْرٰى ﴿۳۹﴾

39. Kwamba habebi mbebaji mzigo wa mwingine;

وَاَنْ لَّيْسَ لِلْاِنْسَانِ اِلَّا مَا سَعٰى ﴿۴۰﴾

40. Na mtu hatapata ila aliyoyafanyia juhudi;

وَاَنَّ سَعْيَهٗ سَوْفَ يُرٰى ﴿۴۱﴾

41. Na ya kwamba juhudi yake hivi karibuni itaonekana;

ثُمَّ يُجْزٰىهُ الْجَزَآءَ الْاَوْفٰى ﴿۴۲﴾

42. Kisha atalipwa malipo yaliyo kamili;

وَاَنَّ اِلٰى رَبِّكَ الْمُنْتَهٰى ﴿۴۳﴾

43. Na kwamba mwisho ni kwa Mola wako;

وَاَنَّهٗ هُوَ اَضْحَكَ وَاَبْكٰى ﴿۴۴﴾

44. Na kwamba Yeye ndiye anayechekesha na kuliza;

وَاَنَّهٗ هُوَ اَمَاتَ وَاَحْيَا ﴿۴۵﴾

45. Na kwamba Yeye ndiye Afishaye na kuhuisha;

وَاَنَّهٗ خَلَقَ الزَّوْجَيْنِ الذَّكَرَ وَالْاُنْثٰى ﴿۴۶﴾

46. Na kwamba Yeye ndiye Aumbaye jozi ya kiume na kike;

Aya 33. *Ambao wanajiepusha na madhambi makuu.* Madhambi makuu ni saba: (1) *Shirk*, yaani kuweka mungu mwingine pamoja na Allah; (2) zinaa; (3) kuua; (4) kusema uwongo; (5) kumwasi mama na baba; (6) kumsingizia mwanamke mwaminifu; (7) kutoroka katika Jihadi kwa kuwahofu makafiri. Kadhalika dhambi kubwa ni yo yote ambayo mtu ameizoea sana na anaona taabu kuiacha.

مِنْ نُّطْفَةٍ اِذَا تُمْنٰى ﴿٤٧﴾

47. Katika mbegu ya uzazi inapotiwa;

وَاَنَّ عَلَيْهِ النَّشْاَةَ الْاُخْرٰى ﴿٤٨﴾

48. Na kwamba juu Yake ni ufufuo mwingine;

وَاَنَّهٗ هُوَ اَغْنٰى وَاَقْنٰى ﴿٤٩﴾

49. Na kwamba Yeye ndiye Atajirishaye na Atoaye hazina;

وَاَنَّهٗ هُوَ رَبُّ الشِّعْرٰى ﴿٥٠﴾

50. Na kwamba Yeye ndiye Mola wa (nyota) Siraa;

وَاَنَّهٗۤ اَهْلَكَ عَادَا ۨ الْاُوْلٰى ﴿٥١﴾

51. Na kwamba Yeye ndiye Aliyewaangamiza Waadi wa kwanza,

وَثَمُوْدَا فَمَاۤ اَبْقٰى ﴿٥٢﴾

52. Na Wathamudi, Hakuwabakisha,

وَقَوْمَ نُوْحٍ مِّنْ قَبْلُ ؕ اِنَّهُمْ كَانُوْا هُمْ اَظْلَمَ وَاَطْغٰى ﴿٥٣﴾

53. Na kabla yao watu wa Nuhu- hakika wao walikuwa wadhalimu na waasi sana-

وَالْمُؤْتَفِكَةَ اَهْوٰى ﴿٥٤﴾

54. Na hata miji iliyopinduliwa Yeye ndiye Aliyeiangusha.

فَغَشّٰىهَا مَا غَشّٰى ﴿٥٥﴾

55. Basi vikaifunikiza vilivyofunikiza.

فَبِاَيِّ اٰلَآءِ رَبِّكَ تَتَمَارٰى ﴿٥٦﴾

56. Basi juu ya neema gani ya Mola wako utakayobishania?

هٰذَا نَذِيْرٌ مِّنَ النُّذُرِ الْاُوْلٰى ﴿٥٧﴾

57. Huyu Mwonyaji wetu pia ni kama Waonyaji wa zamani.

اَزِفَتِ الْاٰزِفَةُ ﴿٥٨﴾

58. Lenye kukaribia limeshakaribia.

لَيْسَ لَهَا مِنْ دُوْنِ اللّٰهِ كَاشِفَةٌ ﴿٥٩﴾

59. Hakuna awezaye kuliondoa ila Allah.

اَفَمِنْ هٰذَا الْحَدِيْثِ تَعْجَبُوْنَ ﴿٦٠﴾

60. Je! mnaistaajabia hadithi hii?

وَتَضْحَكُوْنَ وَلَا تَبْكُوْنَ ﴿٦١﴾

61. Na mnacheka wala hamlii,

وَاَنْتُمْ سٰمِدُوْنَ ﴿٦٢﴾

62. Na hali ninyi mmeghafilika?

فَاسْجُدُوْا لِلّٰهِ وَاعْبُدُوْا ﴿٦٣﴾ ع ۷ السجدة ۱۲

63. Basi msujudieni Allah na mwabudu.

Aya 63. Baada ya Allah kueleza utukufu Wake na unyonge wa masanamu akaamrisha asujudiwe. Basi iliposhuka Aya hii, wakati huo Mtume *s.a.w.* alikuwa katika kundi la watu na makafiri pia walikuwapo, akaporomoka kumsujudia Allah na waaminio pia wakasujudu; na makafiri nguvu ya maneno ya Kurani ikawafanya nao wasujudu. Tukio hili ndilo lililowafanya akina Wakidi kubuni kisa tulichokieleza hapo juu.

Hii ndiyo Aya ya kwanza inayoamrisha kusujudu na Mtume na masahaba wakasujudu; na kuna Aya zingine katika mahali pengine kumi na tatu zinazoamrisha kusujudu, basi zinaposomwa watu lazima wasujudu.

سُوْرَةُ الْقَمَرِ مَكِّيَّةٌ وَّ هِيَ مَعَ الْبَسْمَلَةِ سِتٌّ وَّ خَمْسُوْنَ اٰيَةً وَّ ثَلَاثَةُ رُكُوْعَاتٍ

54. SURA AL-QAMAR

Imeteremshwa Makka

Ina mafungu 3 na Aya 56 pamoja na Bismillahi

بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ ①

1. Kwa jina la Allah, Mwingi wa rehema, Mwingi wa ukarimu.

اِقْتَرَبَتِ السَّاعَةُ وَانْشَقَّ الْقَمَرُ ②

2. Saa imekaribia na mwezi umepasuka.

وَاِنْ يَّرَوْا اٰيَةً يُّعْرِضُوْا وَيَقُوْلُوْا سِحْرٌ مُّسْتَمِرٌّ ③

3. Na wakiiona Ishara hugeuka upande na husema: Uchawi unaoendelea!

وَكَذَّبُوْا وَاتَّبَعُوْٓا اَهْوَآءَهُمْ وَكُلُّ اَمْرٍ مُّسْتَقِرٌّ ④

4. Na walikadhibisha na wakafuata matamanio yao; na kila jambo limewekwa kwa wakati wake.

وَلَقَدْ جَآءَهُمْ مِّنَ الْاَنْۢبَآءِ مَا فِيْهِ مُزْدَجَرٌ ۙ ⑤

5. Na kwa yakini zimewafikia baadhi ya habari zenye makatazo makubwa.

حِكْمَةٌۢ بَالِغَةٌ فَمَا تُغْنِ النُّذُرُ ۙ ⑥

6. (Zenye) Hekima kamili, lakini maonyo (kwao) hayafai;

فَتَوَلَّ عَنْهُمْ ۘ يَوْمَ يَدْعُ الدَّاعِ اِلٰى شَيْءٍ نُّكُرٍ ۙ ⑦

7. Hivyo ujiepushe nao. Siku atakapoita mwitaji kwenye jambo lisilopendeza mno,

خُشَّعًا اَبْصَارُهُمْ يَخْرُجُوْنَ مِنَ الْاَجْدَاثِ كَاَنَّهُمْ جَرَادٌ مُّنْتَشِرٌ ۙ ⑧

8. Macho yao yatainama kwa dhila; watatoka katika makaburi kama wao n nzige waliotawanyika.

Neno *Mwezi* linalotokea katika Aya 2 ndilo jina la sura hii. Mwezi ulikuwa ni alama ya nguvu ya Waarabu na kupasuka kwake kulikotajwa ni alama ya kuvunjika nguvu yao. Sura hii ilishuka Makka.

Aya 2. *Mwezi umepasuka.* Hii ni mojawapo katika Ishara alizoonyesha Mtume Muhammad *s.a.w.* Toka kabla ya Uislamu Waarabu walikuwa na masimulizi ya kuwa nguvu yao itavunjika na mamlaka mpya itatawala, na alama yake itakuwa mwezi utapasuka. Basi siku moja Mtume *s.a.w.* alikuwa amekaa usiku akiwaeleza habari za ujumbe wake Waarabu wanaoabudu masanamu, na Waislamu wachache walikuwapo. Waabuduo masanamu wakamwambia aonyeshe Ishara. Akawaambia: Tazameni mwezi umepasuka. Na wakaona kweli umepasuka. Hii ilikuwa kuwakumbusha ya kuwa habari mlizoambiwa zamani sasa ndiyo zinatimia na ni juu yenu kukubali Uislamu. Na baadaye ilitimia bishara hii, nguvu ya Waarabu na wafalme ilivunjika na mahala pake ukasimama ufalme wa Kiislamu.

مُّهۡطِعِيۡنَ اِلَى الدَّاعِ ؕ يَقُوۡلُ الۡكٰفِرُوۡنَ هٰذَا يَوۡمٌ عَسِرٌ ۝٩

9. Wakimkimbilia mwitaji. Watasema makafiri: Siku hii ni siku ngumu.

كَذَّبَتۡ قَبۡلَهُمۡ قَوۡمُ نُوۡحٍ فَكَذَّبُوۡا عَبۡدَنَا وَقَالُوۡا مَجۡنُوۡنٌ وَّازۡدُجِرَ ۝١٠

10. Kabla yao pia watu wa Nuhu walikadhibisha, walimkadhibisha Mtumishi Wetu na wakasema ni majnuni, na akakemewa.

فَدَعَا رَبَّهٗۤ اَنِّىۡ مَغۡلُوۡبٌ فَانۡتَصِرۡ ۝١١

11. Ndipo akamwomba Mola wake: Kwa hakika nimeshindwa, basi Unisaidie.

فَفَتَحۡنَاۤ اَبۡوَابَ السَّمَآءِ بِمَآءٍ مُّنۡهَمِرٍ ۝١٢

12. Mara Tukaifungua milango ya mawingu kwa maji yanayomiminika.

وَّفَجَّرۡنَا الۡاَرۡضَ عُيُوۡنًا فَالۡتَقَى الۡمَآءُ عَلٰۤى اَمۡرٍ قَدۡ قُدِرَ ۝١٣

13. Na Tukazibubujisha chemchem katika ardhi na maji yakakutana juu ya jambo lililokwisha kadiriwa.

وَحَمَلۡنٰهُ عَلٰى ذَاتِ اَلۡوَاحٍ وَّدُسُرٍ ۝١٤

14. Na Tukamchukua juu ya ile iliyotengenezwa kwa mbao na misumari.

تَجۡرِىۡ بِاَعۡيُنِنَا ۚ جَزَآءً لِّمَنۡ كَانَ كُفِرَ ۝١٥

15. Ikaenda mbele ya macho Yetu: ni tuzo kwa yule aliyekuwa amekataliwa.

وَلَقَدۡ تَّرَكۡنٰهَاۤ اٰيَةً فَهَلۡ مِنۡ مُّدَّكِرٍ ۝١٦

16. Na kwa yakini Tuliiacha iwe Ishara, lakini je, yuko anayekumbuka?

فَكَيۡفَ كَانَ عَذَابِىۡ وَنُذُرِ ۝١٧

17. Basi ilikuwaje adhabu Yangu na maonyo Yangu!

وَلَقَدۡ يَسَّرۡنَا الۡقُرۡاٰنَ لِلذِّكۡرِ فَهَلۡ مِنۡ مُّدَّكِرٍ ۝١٨

18. Na kwa yakini Tumeifanya Kurani kuwa nyepesi kuikumbuka , lakini je, yuko anayeikumbuka?

كَذَّبَتۡ عَادٌ فَكَيۡفَ كَانَ عَذَابِىۡ وَنُذُرِ ۝١٩

19. Waadi walikadhibisha, basi ilikuwaje adhabu Yangu na maonyo Yangu!

اِنَّاۤ اَرۡسَلۡنَا عَلَيۡهِمۡ رِيۡحًا صَرۡصَرًا فِىۡ يَوۡمِ نَحۡسٍ مُّسۡتَمِرٍّ ۝٢٠

20. Hakika Tuliwapelekea upepo mkali katika siku ya nuksi iendeleayo,

تَنۡزِعُ النَّاسَ ۙ كَاَنَّهُمۡ اَعۡجَازُ نَخۡلٍ مُّنۡقَعِرٍ ۝٢١

21. Ukiwaangusha watu kana kwamba ni magogo ya mitende yaliyong'olewa.

فَكَيۡفَ كَانَ عَذَابِىۡ وَنُذُرِ ۝٢٢

22. Basi ilikuwaje adhabu Yangu na maonyo Yangu!

وَلَقَدْ يَسَّرْنَا الْقُرْاٰنَ لِلذِّكْرِ فَهَلْ مِنْ مُّدَّكِرٍ ﴿٢٣﴾ ع ٨

23. Na kwa yakini Tumeifanya Kurani kuwa nyepesi kuikumbuka, lakini je, yuko anayeikumbuka?

FUNGU 2

كَذَّبَتْ ثَمُوْدُ بِالنُّذُرِ ﴿٢٤﴾

24. Wathamudi waliwakadhibisha Waonyaji.

فَقَالُوْٓا اَبَشَرًا مِّنَّا وَاحِدًا نَّتَّبِعُهٗٓ ۙ اِنَّآ اِذًا لَّفِيْ ضَلٰلٍ وَّسُعُرٍ ﴿٢٥﴾

25. Na wakasema: Je, tumfuate mtu mmoja miongoni mwetu! Kwa hakika ndipo tutakuwa katika upotevu na uwendawazimu.

ءَاُلْقِيَ الذِّكْرُ عَلَيْهِ مِنْۢ بَيْنِنَا بَلْ هُوَ كَذَّابٌ اَشِرٌ ﴿٢٦﴾

26. Je, yeye ameteremshiwa ukumbusho kati yetu? Bali yeye ni mwongo mkubwa, ajivunaye.

سَيَعْلَمُوْنَ غَدًا مَّنِ الْكَذَّابُ الْاَشِرُ ﴿٢٧﴾

27. Watajua kesho ni nani mwongo mkubwa ajivunaye.

اِنَّا مُرْسِلُوا النَّاقَةِ فِتْنَةً لَّهُمْ فَارْتَقِبْهُمْ وَاصْطَبِرْ ﴿٢٨﴾

28. Kwa yakini Tutampeleka ngamia jike ili kuwajaribu, basi uwaangalie na ufanye subira.

وَنَبِّئْهُمْ اَنَّ الْمَآءَ قِسْمَةٌۢ بَيْنَهُمْ ۚ كُلُّ شِرْبٍ مُّحْتَضَرٌ ﴿٢٩﴾

29. Na waambie kwamba maji hayo yamegawanywa baina yao, kila wakati uliopangwa kwa ajili ya kunywa ni lazima ufuatwe.

فَنَادَوْا صَاحِبَهُمْ فَتَعَاطٰى فَعَقَرَ ﴿٣٠﴾

30. Lakini wakamwita rafiki yao, na akamkamata (ngamia huyo), na akamkata miguu.

فَكَيْفَ كَانَ عَذَابِيْ وَنُذُرِ ﴿٣١﴾

31. Basi ilikuwaje adhabu Yangu na maonyo Yangu!

اِنَّآ اَرْسَلْنَا عَلَيْهِمْ صَيْحَةً وَّاحِدَةً فَكَانُوْا كَهَشِيْمِ الْمُحْتَظِرِ ﴿٣٢﴾

32. Kwa yakini Tuliwapelekea mngurumo mmoja tu, basi wakawa kama majani makavu yaliyosagika.

وَلَقَدْ يَسَّرْنَا الْقُرْاٰنَ لِلذِّكْرِ فَهَلْ مِنْ مُّدَّكِرٍ ﴿٣٣﴾

33. Na kwa yakini Tumeifanya Kurani kuwa nyepesi kuikumbuka, lakini je, yuko anayekumbuka?

كَذَّبَتْ قَوْمُ لُوْطٍ بِالنُّذُرِ ﴿٣٤﴾

34. Watu wa Luti waliwakadhibisha Waonyaji.

35. Hakika Sisi Tuliwapelekea tufani ya mawe isipokuwa wafuasi wa Luti, Tukawaokoa karibu na alfajiri,

اِنَّآ اَرۡسَلۡنَا عَلَيۡهِمۡ حَاصِبًا اِلَّآ اٰلَ لُوۡطٍ ؕ نَجَّيۡنٰهُمۡ بِسَحَرٍ ۙ﴿۳۵﴾

36. Kwa neema iliyotoka Kwetu; hivyo ndivyo Tumlipavyo anayeshukuru.

نِّعۡمَةً مِّنۡ عِنۡدِنَا ؕ كَذٰلِكَ نَجۡزِىۡ مَنۡ شَكَرَ ﴿۳۶﴾

37. Na kwa hakika yeye aliwaogopesha mkamato Wetu, lakini wao wakabishana na Waonyaji.

وَلَقَدۡ اَنۡذَرَهُمۡ بَطۡشَتَنَا فَتَمَارَوۡا بِالنُّذُرِ ﴿۳۷﴾

38. Na wakamtaka asiwaangalie wageni wake, ndipo Tukayapofusha macho yao; basi onjeni adhabu Yangu na maonyo Yangu.

وَلَقَدۡ رَاوَدُوۡهُ عَنۡ ضَيۡفِهٖ فَطَمَسۡنَآ اَعۡيُنَهُمۡ فَذُوۡقُوۡا عَذَابِىۡ وَنُذُرِ ﴿۳۸﴾

39. Na kwa hakika adhabu iendeleayo ikawafikia asubuhi.

وَلَقَدۡ صَبَّحَهُمۡ بُكۡرَةً عَذَابٌ مُّسۡتَقِرٌّ ۚ﴿۳۹﴾

40. Basi onjeni adhabu Yangu na maonyo Yangu.

فَذُوۡقُوۡا عَذَابِىۡ وَنُذُرِ ﴿۴۰﴾

41. Na kwa yakini Tumeifanya Kurani kuwa nyepesi kuikumbuka, lakini je, yuko anayekumbuka?

وَلَقَدۡ يَسَّرۡنَا الۡقُرۡاٰنَ لِلذِّكۡرِ فَهَلۡ مِنۡ مُّدَّكِرٍ ﴿۴۱﴾ ع ۱۸/۹

FUNGU 3

42. Na kwa kweli Waonyaji waliwafikia watu wa Firauni.

وَلَقَدۡ جَآءَ اٰلَ فِرۡعَوۡنَ النُّذُرُ ۚ﴿۴۲﴾

43. Wakakadhibisha Ishara Zetu zote, kwa hiyo Tukawakamata kwa mkamato wa Mwenye nguvu, Mwenye uwezo.

كَذَّبُوۡا بِاٰيٰتِنَا كُلِّهَا فَاَخَذۡنٰهُمۡ اَخۡذَ عَزِيۡزٍ مُّقۡتَدِرٍ ﴿۴۲﴾

44. Je, makafiri wenu ni bora kuliko hao, au je, yameandikwa vitabuni kwamba ninyi mtaachwa?

اَكُفَّارُكُمۡ خَيۡرٌ مِّنۡ اُولٰٓئِكُمۡ اَمۡ لَكُمۡ بَرَآءَةٌ فِى الزُّبُرِ ۚ﴿۴۳﴾

45. Au je, wanasema, Sisi ni jamii ya watu tuwezao kulipiza kisasi?

اَمۡ يَقُوۡلُوۡنَ نَحۡنُ جَمِيۡعٌ مُّنۡتَصِرٌ ﴿۴۵﴾

46. (Lakini) jamii hiyo karibu itashindwa na watageuza migongo.

سَيُهۡزَمُ الۡجَمۡعُ وَيُوَلُّوۡنَ الدُّبُرَ ﴿۴۶﴾

Aya 46. Katika siku ya vita vya Badri Mtume *s.a.w.* alisali katika hema lake akiomba, "Ee Mola wangu, ninakusihi juu ya agano Lako na ahadi Yako; Ee Mola, ukiacha kikundi hiki

47. Walakini saa ile ni wakati wao walioahidiwa, na saa hiyo ni nzito sana na chungu sana.

بَلِ السَّاعَةُ مَوْعِدُهُمْ وَالسَّاعَةُ اَدْهٰى وَاَمَرُّ ﴿٤٦﴾

48. Bila shaka wakosefu wamo katika upotevu na uwendawazimu.

اِنَّ الْمُجْرِمِيْنَ فِيْ ضَلٰلٍ وَّسُعُرٍ ﴿٤٧﴾

49. Siku watakayokokotwa Motoni kifudifudi: Onjeni mguso wa Jahanamu.

يَوْمَ يُسْحَبُوْنَ فِي النَّارِ عَلٰى وُجُوْهِهِمْ ذُوْقُوْا مَسَّ سَقَرَ ﴿٤٨﴾

50. Kwa hakika Sisi Tumekiumba kila kitu kwa kipimo.

اِنَّا كُلَّ شَيْءٍ خَلَقْنٰهُ بِقَدَرٍ ﴿٤٩﴾

51. Na haiwi amri Yetu ila moja tu (ifikayo) kama kukapua macho.

وَمَآ اَمْرُنَآ اِلَّا وَاحِدَةٌ كَلَمْحٍ بِالْبَصَرِ ﴿٥٠﴾

52. Na kwa yakini Tumekwisha waangamiza wenzenu; lakini je, yuko anayekumbuka?

وَلَقَدْ اَهْلَكْنَآ اَشْيَاعَكُمْ فَهَلْ مِنْ مُّدَّكِرٍ ﴿٥١﴾

53. Na kila jambo walifanyalo limo ndani ya Misahafu.

وَكُلُّ شَيْءٍ فَعَلُوْهُ فِي الزُّبُرِ ﴿٥٢﴾

54. Na kila kidogo na kikubwa kimeandikwa.

وَكُلُّ صَغِيْرٍ وَّكَبِيْرٍ مُّسْتَطَرٌ ﴿٥٣﴾

55. Bila shaka wamchao Allah watakuwa katika Mabustani na mito.

اِنَّ الْمُتَّقِيْنَ فِيْ جَنّٰتٍ وَّنَهَرٍ ﴿٥٤﴾

56. Katika makao mazuri karibu na Mfalme mwenye uwezo.

فِيْ مَقْعَدِ صِدْقٍ عِنْدَ مَلِيْكٍ مُّقْتَدِرٍ ﴿٥٥﴾ ع ٢ ١٠

---

kiangamie basi hutaabudiwa tena duniani." Seyidna Abu Bakar alimshika mkono na akamwambia, "Mungu anakutoshea, Ee Mtume wa Mungu." Basi Mtume *s.a.w.* akatoka na kusoma Aya hizi, *"Jamii hiyo karibu itashindwa na watageuza migongo. Walakini saa ile ni wakati wao walioahidiwa, na saa ile ni nzito sana na chungu sana."* (Bukhari) Jambo hili linaonyesha ya kuwa Mtume na masahaba wake walikuwa wakifahamu barabara kuwa Aya hizi ni bishara zinazotabiri matokeo yatakayokuja tokea. Na mambo yote yaliyotajwa katika Aya hizi yalitokea katika vita vya Badri.

سُوْرَةُ الرَّحْمٰنِ مَكِّيَّةٌ وَّ هِيَ مَعَ الْبَسْمَلَةِ تِسْعٌ وَّ سَبْعُوْنَ اٰيَةً وَّ ثَلَاثَةُ رُكُوْعَاتٍ

55. SURA AR-RAHMAAN

Imeteremshwa Makka

Ina mafungu 3 na Aya 79 pamoja na Bismillahi

بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ ①

1. Kwa jina la Allah, Mwingi wa rehema, Mwingi wa ukarimu.

اَلرَّحْمٰنُ ۙ ②

2. Mwingi wa rehema,

عَلَّمَ الْقُرْاٰنَ ؕ ③

3. Amefundisha Kurani.

خَلَقَ الْاِنْسَانَ ۙ ④

4. Amemwumba mtu,

عَلَّمَهُ الْبَيَانَ ⑤

5. Akamfundisha ustadi wa kujieleza.

اَلشَّمْسُ وَالْقَمَرُ بِحُسْبَانٍ ۬ ⑥

6. Jua na mwezi (huenda) kwa hesabu.

وَّالنَّجْمُ وَالشَّجَرُ يَسْجُدٰنِ ⑦

7. Na miche na miti vinasujudu.

وَالسَّمَآءَ رَفَعَهَا وَوَضَعَ الْمِيْزَانَ ۙ ⑧

8. Na mbingu Ameziinua na Akaweka mizani.

اَلَّا تَطْغَوْا فِي الْمِيْزَانِ ⑨

9. Ili msikose katika mizani.

وَاَقِيْمُوا الْوَزْنَ بِالْقِسْطِ وَلَا تُخْسِرُوا الْمِيْزَانَ ⑩

10. Na pimeni kipimo kwa haki wala msipunguze mizani.

وَالْاَرْضَ وَضَعَهَا لِلْاَنَامِ ۙ ⑪

11. Na ardhi Ameitandaza kwa ajili ya viumbe.

فِيْهَا فَاكِهَةٌ ۙ وَّالنَّخْلُ ذَاتُ الْاَكْمَامِ ۙ ⑫

12. Humo yamo matunda na mitende yenye matumba.

وَالْحَبُّ ذُو الْعَصْفِ وَالرَّيْحَانُ ۚ ⑬

13. Na punje zenye makapi na mimea yenye harufu nzuri.

Jina la sura hii ni la Allah, *Ar-Rahmaan* ambalo linatokea katika Aya ya 2, na sura nzima inaeleza juu ya neema za Allah. Sura hii ilishuka Makka.

Aya 2. *Ar-Rahmaan,* "Mwingi wa rehema." Neno hili limeelezwa katika sura ya kwanza.

Aya 4. *Al-Insaan,* "Mtu." Neno hili limefasiriwa na mufasirina wengi kwa maana ya *mwanadamu kamili* yaani Mtume Muhammad *s.a.w.*

فَبِاَيِّ اٰلَآءِ رَبِّكُمَا تُكَذِّبٰنِ ﴿١٤﴾

14. Basi (Enyi Majini na Watu) ninyi wawili mtakataa neema gani za Mola wenu?

خَلَقَ الْاِنْسَانَ مِنْ صَلْصَالٍ كَالْفَخَّارِ ﴿١٥﴾

15. Ameumba mtu kwa udongo wa mfinyanzi (utoao sauti) kama vyombo vilivyookwa.

وَخَلَقَ الْجَآنَّ مِنْ مَّارِجٍ مِّنْ نَّارٍ ﴿١٦﴾

16. Na Akaumba majinni kwa miale ya moto.

فَبِاَيِّ اٰلَآءِ رَبِّكُمَا تُكَذِّبٰنِ ﴿١٧﴾

17. Basi ninyi wawili mtakataa neema gani za Mola wenu?

رَبُّ الْمَشْرِقَيْنِ وَرَبُّ الْمَغْرِبَيْنِ ﴿١٨﴾

18. Mola wa mashariki mbili na Mola wa magharibi mbili.

فَبِاَيِّ اٰلَآءِ رَبِّكُمَا تُكَذِّبٰنِ ﴿١٩﴾

19. Basi ninyi wawili mtakataa neema gani za Mola wenu?

مَرَجَ الْبَحْرَيْنِ يَلْتَقِيٰنِ ﴿٢٠﴾

20. Bila shaka Atazichanganya bahari mbili kwa kuzikutanisha.

بَيْنَهُمَا بَرْزَخٌ لَّا يَبْغِيٰنِ ﴿٢١﴾

21. Baina yao pana ukingo haziuvuki.

فَبِاَيِّ اٰلَآءِ رَبِّكُمَا تُكَذِّبٰنِ ﴿٢٢﴾

22. Basi ninyi wawili mtakataa neema gani za Mola wenu?

يَخْرُجُ مِنْهُمَا اللُّؤْلُؤُ وَالْمَرْجَانُ ﴿٢٣﴾

23. Katika hizo mbili hutoka lulu na marijani.

فَبِاَيِّ اٰلَآءِ رَبِّكُمَا تُكَذِّبٰنِ ﴿٢٤﴾

24. Basi ninyi wawili mtakataa neema gani za Mola wenu?

وَلَهُ الْجَوَارِ الْمُنْشَاٰتُ فِي الْبَحْرِ كَالْاَعْلَامِ ﴿٢٥﴾

25. Na majahazi ni Yake yaliyoinuka baharini kama milima.

فَبِاَيِّ اٰلَآءِ رَبِّكُمَا تُكَذِّبٰنِ ﴿٢٦﴾

26. Basi ninyi wawili mtakataa neema gani za Mola wenu?

FUNGU 2

كُلُّ مَنْ عَلَيْهَا فَانٍ ﴿٢٧﴾

27. Kila kilichoko juu yake kitatoweka,

Aya 14. *Ninyi wawili,* yumkini muradi hapa ni kama ilivyo katika Aya ya 34 ya sura hii, yaani *Jinn* na *Ins* (watu wakubwa na watu wa kawaida). Lakini kwa desturi ya lugha ya Kiarabu maneno wanayoambiwa watu wengi yanapotaka kutiwa mkazo hutamkwa katika jinsi ya uwili.

Aya 20. *Zikutane.* Bishara hii imekwisha timia. Bahari ya Sham na ya Mediterranneo zimekutanishwa na mfereji mkubwa wa Suez, na kadhalika bahari ya Atlantic na Pacific zimekutanishwa na mfereji mkubwa wa Panama.

28. Na itabaki dhati ya Mola wako, Mwenye utukufu na heshima.

وَّيَبْقٰى وَجْهُ رَبِّكَ ذُو الْجَلٰلِ وَالْاِكْرَامِ ﴿٢٨﴾

29. Basi ninyi wawili mtakataa neema gani za Mola wenu?

فَبِاَيِّ اٰلَآءِ رَبِّكُمَا تُكَذِّبٰنِ ﴿٢٩﴾

30. Humwomba Yeye kila kilichomo mbinguni na ardhini; kila wakati Yeye Anakuwa katika shani mpya.

يَسْـَٔلُهٗ مَنْ فِي السَّمٰوٰتِ وَالْاَرْضِ ؕ كُلَّ يَوْمٍ هُوَ فِيْ شَاْنٍ ﴿٣٠﴾

31. Basi ninyi wawili mtakataa neema gani za Mola wenu?

فَبِاَيِّ اٰلَآءِ رَبِّكُمَا تُكَذِّبٰنِ ﴿٣١﴾

32. Karibu Tutawaelekeeni, enyi majeshi mawili yenye nguvu!

سَنَفْرُغُ لَكُمْ اَيُّهَ الثَّقَلٰنِ ﴿٣٢﴾

33. Basi ninyi wawili mtakataa neema gani za Mola wenu?

فَبِاَيِّ اٰلَآءِ رَبِّكُمَا تُكَذِّبٰنِ ﴿٣٣﴾

34. Enyi jamii ya majinni na watu, kama mkiweza kutoka nje ya mipaka ya mbingu na ardhi, basi tokeni; lakini hamtatoka ila kwa idhini.

يٰمَعْشَرَ الْجِنِّ وَالْاِنْسِ اِنِ اسْتَطَعْتُمْ اَنْ تَنْفُذُوْا مِنْ اَقْطَارِ السَّمٰوٰتِ وَالْاَرْضِ فَانْفُذُوْا ؕ لَا تَنْفُذُوْنَ اِلَّا بِسُلْطٰنٍ ﴿٣٤﴾

35. Basi ninyi wawili mtakataa neema gani za Mola wenu?

فَبِاَيِّ اٰلَآءِ رَبِّكُمَا تُكَذِّبٰنِ ﴿٣٥﴾

36. Mtashushiwa miale ya moto na moshi wa aina fulani basi nyinyi wawili hamtaweza kulipa kisasi.

يُرْسَلُ عَلَيْكُمَا شُوَاظٌ مِّنْ نَّارٍ ۙ وَّنُحَاسٌ فَلَا تَنْتَصِرٰنِ ﴿٣٦﴾

37. Basi ninyi wawili mtakataa neema gani za Mola wenu?

فَبِاَيِّ اٰلَآءِ رَبِّكُمَا تُكَذِّبٰنِ ﴿٣٧﴾

38. Na zitakapopasuka mbingu zitakuwa nyekundu kama ngozi nyekundu.

فَاِذَا انْشَقَّتِ السَّمَآءُ فَكَانَتْ وَرْدَةً كَالدِّهَانِ ﴿٣٨﴾

39. Basi ninyi wawili mtakataa neema gani za Mola wenu?

فَبِاَيِّ اٰلَآءِ رَبِّكُمَا تُكَذِّبٰنِ ﴿٣٩﴾

40. Basi siku hiyo hataulizwa kwa dhambi zake mtu wala jinni.

فَيَوْمَئِذٍ لَّا يُسْـَٔلُ عَنْ ذَنْۢبِهٖٓ اِنْسٌ وَّلَا جَآنٌّ ﴿٤٠﴾

41. Basi ninyi wawili mtakataa neema gani za Mola wenu?

فَبِاَيِّ اٰلَآءِ رَبِّكُمَا تُكَذِّبٰنِ ﴿٤١﴾

Aya 30. Yaum, "Siku," muradi wake ni kila wakati, kila saa na kila dakika. *Anakuwa katika shani,* yaani anaonyesha maonyesho mbalimbali: anaghofiri dhambi na pengine anaondoa msiba, na anawainua watu na anawadhalilisha wengine (Bukhari).

يُعْرَفُ الْمُجْرِمُوْنَ بِسِيْمٰهُمْ فَيُؤْخَذُ بِالنَّوَاصِيْ وَالْاَقْدَامِ ﴿٤٢﴾

42. Watajulikana wakosefu kwa alama zao, basi watakamatwa kwa nywele za mapaji na kwa miguu.

فَبِاَيِّ اٰلَآءِ رَبِّكُمَا تُكَذِّبٰنِ ﴿٤٣﴾

43. Basi ninyi wawili mtakataa neema gani za Mola wenu?

هٰذِهٖ جَهَنَّمُ الَّتِيْ يُكَذِّبُ بِهَا الْمُجْرِمُوْنَ ﴿٤٤﴾

44. Hii ndiyo Jahanamu ambayo wakosefu wanaikadhibisha.

يَطُوْفُوْنَ بَيْنَهَا وَبَيْنَ حَمِيْمٍ اٰنٍ ﴿٤٥﴾

45. Watakuwa wakizunguka kati yake na kati ya maji ya moto yachemkayo.

فَبِاَيِّ اٰلَآءِ رَبِّكُمَا تُكَذِّبٰنِ ﴿٤٦﴾

46. Basi ninyi wawili mtakataa neema gani za Mola wenu?

FUNGU 3

وَلِمَنْ خَافَ مَقَامَ رَبِّهٖ جَنَّتٰنِ ﴿٤٧﴾

47. Na anayeogopa makamu ya Mola wake, atapata Bustani mbili.

فَبِاَيِّ اٰلَآءِ رَبِّكُمَا تُكَذِّبٰنِ ﴿٤٨﴾

48. Basi ninyi wawili mtakataa neema gani za Mola wenu?

ذَوَاتَآ اَفْنَانٍ ﴿٤٩﴾

49. Zote mbili zikiwa na matawi mengi.

فَبِاَيِّ اٰلَآءِ رَبِّكُمَا تُكَذِّبٰنِ ﴿٥٠﴾

50. Basi ninyi wawili mtakataa neema gani za Mola wenu?

فِيْهِمَا عَيْنٰنِ تَجْرِيٰنِ ﴿٥١﴾

51. Zimo chemchem mbili zinazopita.

فَبِاَيِّ اٰلَآءِ رَبِّكُمَا تُكَذِّبٰنِ ﴿٥٢﴾

52. Basi ninyi wawili mtakataa neema gani za Mola wenu?

فِيْهِمَا مِنْ كُلِّ فَاكِهَةٍ زَوْجٰنِ ﴿٥٣﴾

53. Yamo matunda namna mbili ya kila aina.

فَبِاَيِّ اٰلَآءِ رَبِّكُمَا تُكَذِّبٰنِ ﴿٥٤﴾

54. Basi ninyi wawili mtakataa neema gani za Mola wenu?

مُتَّكِـِٕيْنَ عَلٰى فُرُشٍ بَطَآئِنُهَا مِنْ اِسْتَبْرَقٍ ؕ وَجَنَا الْجَنَّتَيْنِ دَانٍ ﴿٥٥﴾

55. Wakiegemea vitanda ambavyo bitana zake ni za hariri iliyonakishiwa; na matunda yaliyoiva ya Bustani zote mbili yameinamia chini kutokana na uzito.

Aya 47. Pia Aya hii inaweza kufasiriwa, Allah atampa Pepo mbili mtu mwenye kuogopa heshima Yake.

فَبِاَيِّ اٰلَآءِ رَبِّكُمَا تُكَذِّبٰنِ ﴿٥٦﴾

56. Basi ninyi wawili mtakataa neema gani za Mola wenu?

فِيْهِنَّ قٰصِرٰتُ الطَّرْفِ ۙ لَمْ يَطْمِثْهُنَّ اِنْسٌ قَبْلَهُمْ وَلَا جَآنٌّ ﴿٥٧﴾

57. Wamo humo wanawake bikira watulizao macho, mtu ye yote hajawagusa kabla yao (hao watu wa Peponi) wala jinni.

فَبِاَيِّ اٰلَآءِ رَبِّكُمَا تُكَذِّبٰنِ ﴿٥٨﴾

58. Basi ninyi wawili mtakataa neema gani za Mola wenu?

كَاَنَّهُنَّ الْيَاقُوْتُ وَالْمَرْجَانُ ﴿٥٩﴾

59. Kana kwamba wao ni yakuti na marijani.

فَبِاَيِّ اٰلَآءِ رَبِّكُمَا تُكَذِّبٰنِ ﴿٦٠﴾

60. Basi ninyi wawili mtakataa neema gani za Mola wenu?

هَلْ جَزَآءُ الْاِحْسَانِ اِلَّا الْاِحْسَانُ ﴿٦١﴾

61. Hakuna malipo ya ihsani ila ni ihsani.

فَبِاَيِّ اٰلَآءِ رَبِّكُمَا تُكَذِّبٰنِ ﴿٦٢﴾

62. Basi ninyi wawili mtakataa neema gani za Mola wenu?

وَمِنْ دُوْنِهِمَا جَنَّتٰنِ ﴿٦٣﴾

63. Na zaidi ya hizo mbili ziko Bustani mbili nyingine.

فَبِاَيِّ اٰلَآءِ رَبِّكُمَا تُكَذِّبٰنِ ﴿٦٤﴾

64. Basi ninyi wawili mtakataa neema gani za Mola wenu?

مُدْهَآمَّتٰنِ ﴿٦٥﴾

65. Zenye rangi nzuri ya kijani kilichoiva.

فَبِاَيِّ اٰلَآءِ رَبِّكُمَا تُكَذِّبٰنِ ﴿٦٦﴾

66. Basi ninyi wawili mtakataa neema gani za Mola wenu?

فِيْهِمَا عَيْنٰنِ نَضَّاخَتٰنِ ﴿٦٧﴾

67. Zimo chemchem mbili zinazofoka.

فَبِاَيِّ اٰلَآءِ رَبِّكُمَا تُكَذِّبٰنِ ﴿٦٨﴾

68. Basi ninyi wawili mtakataa neema gani za Mola wenu?

فِيْهِمَا فَاكِهَةٌ وَّنَخْلٌ وَّرُمَّانٌ ﴿٦٩﴾

69. Yamo humo matunda na mitende na makomamanga.

Aya 61. Hapa Allah anaeleza ya kuwa amewafanyia watu ihsani nyingi zisizo na idadi na sasa ni juu yao kulipa ihsani. Na Mtume *s.a.w.* amesema, kufanya ihsani kwa Allah ni kumwabudu kama unayemwona (Bukhari). Sio mradi wake ya kuwa Mungu ana haja ya wema wetu, bali jambo hili litafanya ihsani ya Mungu izidi kuwafikia watu kwa namna iliyo bora zaidi. Waidha pia Aya hii inatufunza ya kuwa ni juu yetu kulipa mema tunapotendewa mema na watu.

فَبِاَيِّ اٰلَآءِ رَبِّكُمَا تُكَذِّبٰنِ ۚ﴿٧٠﴾

70. Basi ninyi wawili mtakataa neema gani za Mola wenu?

فِيْهِنَّ خَيْرٰتٌ حِسَانٌ ۚ﴿٧١﴾

71. Wamo humo wanawake wema, wazuri.

فَبِاَيِّ اٰلَآءِ رَبِّكُمَا تُكَذِّبٰنِ ۚ﴿٧٢﴾

72. Basi ninyi wawili mtakataa neema gani za Mola wenu?

حُوْرٌ مَّقْصُوْرٰتٌ فِي الْخِيَامِ ۚ﴿٧٣﴾

73. Weupe wanaotawishwā mahemani.

فَبِاَيِّ اٰلَآءِ رَبِّكُمَا تُكَذِّبٰنِ ۚ﴿٧٤﴾

74. Basi ninyi wawili mtakataa neema gani za Mola wenu?

لَمْ يَطْمِثْهُنَّ اِنْسٌ قَبْلَهُمْ وَلَا جَآنٌّ ۚ﴿٧٥﴾

75. Hajawagusa mtu ye yote kabla yao (watu wa Peponi) wala jinni.

فَبِاَيِّ اٰلَآءِ رَبِّكُمَا تُكَذِّبٰنِ ۚ﴿٧٦﴾

76. Basi ninyi wawili mtakataa neema gani za Mola wenu?

مُتَّكِـِٕيْنَ عَلٰى رَفْرَفٍ خُضْرٍ وَّعَبْقَرِيٍّ حِسَانٍ ۚ﴿٧٧﴾

77. Watayaegemea matakia mazuri sana ya kijani na mazulia bora.

فَبِاَيِّ اٰلَآءِ رَبِّكُمَا تُكَذِّبٰنِ ﴿٧٨﴾

78. Basi ninyi wawili mtakataa neema gani za Mola wenu?

تَبٰرَكَ اسْمُ رَبِّكَ ذِي الْجَلٰلِ وَالْاِكْرَامِ ﴿٧٩﴾ ع ٣ ١٣

79. Ni lenye mibaraka jina la Mola wako Mwenye adhama na heshima.

سُوْرَةُ الْوَاقِعَةِ مَكِّيَّةٌ وَّ هِيَ مَعَ الْبَسْمَلَةِ سَبْعٌ وَّ تِسْعُوْنَ اٰيَةً وَّ ثَلَاثَةُ رُكُوْعَاتٍ

56. SURA AL-WAAQI'A

Imeteremshwa Makka

Ina mafungu 3 na Aya 97 pamoja na Bismillahi

بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ ①

1. Kwa jina la Allah, Mwingi wa rehema, Mwingi wa ukarimu.

اِذَا وَقَعَتِ الْوَاقِعَةُ ②

2. Litakapotokea tukio lenye kutokea,

لَيْسَ لِوَقْعَتِهَا كَاذِبَةٌ ③ وقف لازم

3. Hakuna (nafsi yoyote) itakayoweza kukadhibisha kutokea kwake,

خَافِضَةٌ رَّافِعَةٌ ④

4. Litawafedhehesha (baadhi) na litawatukuza (baadhi),

اِذَا رُجَّتِ الْاَرْضُ رَجًّا ⑤

5. Ardhi itakapotetemeshwa tetemesho,

وَّبُسَّتِ الْجِبَالُ بَسًّا ⑥

6. Na milima itakaposagika msagiko,

فَكَانَتْ هَبَآءً مُّنْۢبَثًّا ⑦

7. Ndipo itakuwa (kama) mavumbi yanayopeperushwa.

وَّكُنْتُمْ اَزْوَاجًا ثَلٰثَةً ⑧

8. Na ninyi mtakuwa namna tatu:

فَاَصْحٰبُ الْمَيْمَنَةِ ۙ مَآ اَصْحٰبُ الْمَيْمَنَةِ ⑨

9. Na watu wa kuume; Ni nani hao watu wa kuume?

وَاَصْحٰبُ الْمَشْئَمَةِ ۙ مَآ اَصْحٰبُ الْمَشْئَمَةِ ⑩

10. Na watu wa kushoto; Ni nani hao watu wa kushoto?

وَالسّٰبِقُوْنَ السّٰبِقُوْنَ ⑪

11. Na watanguliao watakuwa ni wenye kuwapita wote,

اُولٰٓئِكَ الْمُقَرَّبُوْنَ ⑫

12. Hao ndio wenye ukaribu (na Allah),

فِيْ جَنّٰتِ النَّعِيْمِ ⑬

13. Katika Bustani zenye neema.

ثُلَّةٌ مِّنَ الْاَوَّلِيْنَ ⑭

14. Kundi kubwa toka miongoni mwa watu wa siku za kwanza;

Jina la sura hii linatoka katika Aya ya 2. Sura hii ilishuka Makka.

Aya 2. Tukio lililotajwa hapa ama ni la Kiyama au la kuadhibiwa hapa hapa duniani watu wanaoifanyia haki uadui.

15. Na kundi dogo toka miongoni mwa watu wa siku za mwisho;
وَقَلِيْلٌ مِّنَ الْاٰخِرِيْنَ ﴿١٥﴾

16. Juu ya viti vya fahari vilivyopangwa.
عَلٰى سُرُرٍ مَّوْضُوْنَةٍ ﴿١٦﴾

17. Wataviegemea wakielekeana.
مُّتَّكِـِٕيْنَ عَلَيْهَا مُتَقٰبِلِيْنَ ﴿١٧﴾

18. Watawazunguka-zunguka wavulana (wahudumu) wasiochakaa.
يَطُوْفُ عَلَيْهِمْ وِلْدَانٌ مُّخَلَّدُوْنَ ﴿١٨﴾

19. Wakichukua vikombe na mabirika, na mabakuli ya kinywaji safi.
بِاَكْوَابٍ وَّاَبَارِيْقَ ۙ وَكَاْسٍ مِّنْ مَّعِيْنٍ ﴿١٩﴾

20. Hawatawangwa kichwa kwa kukinywa wala hawatalewa.
لَّا يُصَدَّعُوْنَ عَنْهَا وَلَا يُنْزِفُوْنَ ﴿٢٠﴾

21. Na matunda watakayoyapenda.
وَفَاكِهَةٍ مِّمَّا يَتَخَيَّرُوْنَ ﴿٢١﴾

22. Na nyama za ndege watakazozitamani.
وَلَحْمِ طَيْرٍ مِّمَّا يَشْتَهُوْنَ ﴿٢٢﴾

23. Na wanawake bikira wenye macho ya vikombe,
وَحُوْرٌ عِيْنٌ ﴿٢٣﴾

24. Kama lulu zilizofunikwa .
كَاَمْثَالِ اللُّؤْلُؤِ الْمَكْنُوْنِ ﴿٢٤﴾

25. Ni ujira kwa hayo waliyokuwa wakitenda.
جَزَآءًۢ بِمَا كَانُوْا يَعْمَلُوْنَ ﴿٢٥﴾

26. Hawatasikia humo upuuzi wala maneno ya dhambi.
لَا يَسْمَعُوْنَ فِيْهَا لَغْوًا وَّلَا تَاْثِيْمًا ﴿٢٦﴾

27. Isipokuwa itasemwa: Amani, amani.
اِلَّا قِيْلًا سَلٰمًا سَلٰمًا ﴿٢٧﴾

28. Na watu wa kuume, ni nani hao watu wa kuume?
وَاَصْحٰبُ الْيَمِيْنِ ۙ مَآ اَصْحٰبُ الْيَمِيْنِ ﴿٢٨﴾

29. (Watakuwa) katika mikunazi isiyo na miiba,
فِيْ سِدْرٍ مَّخْضُوْدٍ ﴿٢٩﴾

30. Na migomba ipambwayo na matunda,
وَّطَلْحٍ مَّنْضُوْدٍ ﴿٣٠﴾

31. Na (katika) kivuli kilichotandazwa.
وَّظِلٍّ مَّمْدُوْدٍ ﴿٣١﴾

32. Na maji yapitayo.
وَّمَآءٍ مَّسْكُوْبٍ ﴿٣٢﴾

33. Na matunda mengi;
وَّفَاكِهَةٍ كَثِيْرَةٍ ﴿٣٣﴾

34. Hayakatiki wala hayakatazwi,
لَّا مَقْطُوْعَةٍ وَّلَا مَمْنُوْعَةٍ ﴿٣٤﴾

وَّفُرُشٍ مَّرْفُوْعَةٍ ﴿٣٥﴾

35. Na (katika) vitanda vilivyonyanyuliwa.

اِنَّآ اَنْشَاْنٰهُنَّ اِنْشَآءً ﴿٣٦﴾

36. Kwa yakini Tumewaumba (wenzi wao) kwa umbo bora kabisa.

فَجَعَلْنٰهُنَّ اَبْكَارًا ﴿٣٧﴾

37. Na Tukawafanya wasio na kifani,

عُرُبًا اَتْرَابًا ﴿٣٨﴾

38. Wapendao, (walio) hirimu,

لِّاَصْحٰبِ الْيَمِيْنِ ﴿٣٩﴾ ع ١٤

39. Kwa ajili ya watu wa kuume.

FUNGU 2

ثُلَّةٌ مِّنَ الْاَوَّلِيْنَ ﴿٤٠﴾

40. Jamii kubwa ni miongoni mwa watu wa kwanza.

وَثُلَّةٌ مِّنَ الْاٰخِرِيْنَ ﴿٤١﴾

41. Na jamii kubwa ni miongoni mwa (watu) wa mwisho.

وَاَصْحٰبُ الشِّمَالِ ۙ مَآ اَصْحٰبُ الشِّمَالِ ﴿٤٢﴾

42. Na watu wa kushoto, wata-kuwa namna gani watu wa kushoto!

فِيْ سَمُوْمٍ وَّحَمِيْمٍ ﴿٤٣﴾

43. (Watakuwa) katika upepo wa Moto na maji yachemkayo,

وَّظِلٍّ مِّنْ يَّحْمُوْمٍ ﴿٤٤﴾

44. Na kivuli cha moshi mweusi sana,

لَّا بَارِدٍ وَّلَا كَرِيْمٍ ﴿٤٥﴾

45. Si baridi wala si starehe.

اِنَّهُمْ كَانُوْا قَبْلَ ذٰلِكَ مُتْرَفِيْنَ ﴿٤٦﴾

46. Bila shaka wao walikuwa kabla ya haya wakiishi maisha ya anasa,

وَكَانُوْا يُصِرُّوْنَ عَلَى الْحِنْثِ الْعَظِيْمِ ﴿٤٧﴾

47. Na walikuwa wakishikilia kufanya dhambi kubwa;

وَكَانُوْا يَقُوْلُوْنَ ۙ اَئِذَا مِتْنَا وَكُنَّا تُرَابًا وَّعِظَامًا ءَاِنَّا لَمَبْعُوْثُوْنَ ﴿٤٨﴾

48. Na walikuwa wakisema: Tutakapokufa na kuwa udongo na mifupa, je kweli tutafufuliwa?

اَوَاٰبَآؤُنَا الْاَوَّلُوْنَ ﴿٤٩﴾

49. Au baba zetu wa zamani?

قُلْ اِنَّ الْاَوَّلِيْنَ وَالْاٰخِرِيْنَ ﴿٥٠﴾

50. Sema: Bila shaka wa kwanza na wa mwisho,

لَمَجْمُوْعُوْنَ ۙ اِلٰى مِيْقَاتِ يَوْمٍ مَّعْلُوْمٍ ﴿٥١﴾

51. Watakusanywa kwa wakati uliowekwa katika siku maalumu.

ثُمَّ اِنَّكُمْ اَيُّهَا الضَّآلُّوْنَ الْمُكَذِّبُوْنَ ﴿٥٢﴾

52. Kisha ninyi, enyi mliopotea (na) kukadhibisha,

لَاٰكِلُوْنَ مِنْ شَجَرٍ مِّنْ زَقُّوْمٍ ﴿٥٣﴾

53. Kwa yakini mtaula mti wa Zakkum;

فَمَالِـُٔوْنَ مِنْهَا الْبُطُوْنَ ﴿٥٤﴾

54. Na kwa huo mtajaza matumbo,

فَشٰرِبُوْنَ عَلَيْهِ مِنَ الْحَمِيْمِ ﴿٥٥﴾

55. Na juu yake mtakunywa maji yachemkayo;

فَشٰرِبُوْنَ شُرْبَ الْهِيْمِ ﴿٥٦﴾

56. Tena mtakunywa kama anywavyo ngamia mwenye kiu sana.

هٰذَا نُزُلُهُمْ يَوْمَ الدِّيْنِ ﴿٥٧﴾

57. Hiyo ni karamu yao siku ya malipo.

نَحْنُ خَلَقْنٰكُمْ فَلَوْلَا تُصَدِّقُوْنَ ﴿٥٨﴾

58. Sisi Tuliwaumbeni, basi mbona hamsadiki?

اَفَرَءَيْتُمْ مَّا تُمْنُوْنَ ﴿٥٩﴾

59. Je, mmeiona mbegu ya uzazi mnayoitoneza?

ءَاَنْتُمْ تَخْلُقُوْنَهٗٓ اَمْ نَحْنُ الْخٰلِقُوْنَ ﴿٦٠﴾

60. Je, mnaiumba ninyi au Sisi ndio wenye kuiumba?

نَحْنُ قَدَّرْنَا بَيْنَكُمُ الْمَوْتَ وَمَا نَحْنُ بِمَسْبُوْقِيْنَ ﴿٦١﴾

61. Sisi Tumewawekeeni kati yenu mauti, na Sisi Hatuwezi kushindwa.

عَلٰٓى اَنْ نُّبَدِّلَ اَمْثَالَكُمْ وَنُنْشِئَكُمْ فِيْ مَا لَا تَعْلَمُوْنَ ﴿٦٢﴾

62. Kuzibadili sura zenu na kukuinueni na sura msizozitambua.

وَلَقَدْ عَلِمْتُمُ النَّشْاَةَ الْاُوْلٰى فَلَوْلَا تَذَكَّرُوْنَ ﴿٦٣﴾

63. Na bila shaka ninyi mnalijua umbo la kwanza, basi mbona hamchukui nasaha?

اَفَرَءَيْتُمْ مَّا تَحْرُثُوْنَ ﴿٦٤﴾

64. Je, hebu semeni kuhusiana na mnavyovilima.

ءَاَنْتُمْ تَزْرَعُوْنَهٗٓ اَمْ نَحْنُ الزّٰرِعُوْنَ ﴿٦٥﴾

65. Je, ni ninyi mvioteshavyo au Sisi ndio wenye kuviotesha.

لَوْ نَشَآءُ لَجَعَلْنٰهُ حُطَامًا فَظَلْتُمْ تَفَكَّهُوْنَ ﴿٦٦﴾

66. Kama Tungalitaka Tungaliiangamiza kisha mngebaki tu kunung'unika.

Aya 53. Malipo ya Akhera yatafanana na matendo ya watu hapa duniani. Mwenye kufuata tamaa ya dunia, nayo huleta mwako moyoni atajiona katika Moto. Upotevu ambao ni mahaba ya dunia utaonekana kama mti ulio mchungu sana, na mpotevu atautumia jinsi alivyoupendelea upotevu wake duniani. Mpotevu amkadhibishaye Mjumbe wa Allah atamshabihi yule anywaye maji ya moto akiisha kutumia Zakkum (sura 37:63; 44:44). Pengine neno baya limefananishwa na mti mbaya (sura 14:27).

Aya 58. Allah ndiye anayejua kabisa hali za wanadamu kwa kuwa Yeye Mwenyewe ndiye aliyewaumba. Basi kama amekwisha wawekea mambo ya kustawisha hali ya miili yao anawezaje kuacha kuwatengenezea hali njema kwa ajili ya roho zao?

67. Hakika sisi tumegharimishwa, إِنَّا لَمُغْرَمُونَ ﴿٦٧﴾

68. Bali sisi tumenyimwa. بَلْ نَحْنُ مَحْرُومُونَ ﴿٦٨﴾

69. Je, mmeyaona maji ambayo mnayanywa? أَفَرَءَيْتُمُ الْمَآءَ الَّذِى تَشْرَبُونَ ﴿٦٩﴾

70. Je, mmeyateremsha ninyi toka mawinguni au Sisi ndio wenye kuyateremsha? ءَأَنتُمْ أَنزَلْتُمُوهُ مِنَ الْمُزْنِ أَمْ نَحْنُ الْمُنزِلُونَ ﴿٧٠﴾

71. Tungalipenda Tungaliyafanya makali; basi mbona hamshukuru? لَوْ نَشَآءُ جَعَلْنَٰهُ أُجَاجًا فَلَوْلَا تَشْكُرُونَ ﴿٧١﴾

72. Je, mmeuona moto ambao mnauwasha? أَفَرَءَيْتُمُ النَّارَ الَّتِى تُورُونَ ﴿٧٢﴾

73. Je, mti wake mmeuumba ninyi au Sisi ndio Tuumbao? ءَأَنتُمْ أَنشَأْتُمْ شَجَرَتَهَآ أَمْ نَحْنُ الْمُنشِـُٔونَ ﴿٧٣﴾

74. Sisi Tumeufanya kuwa ukumbusho na manufaa kwa wasafirio. نَحْنُ جَعَلْنَٰهَا تَذْكِرَةً وَمَتَٰعًا لِّلْمُقْوِينَ ﴿٧٤﴾

75. Basi litukuze jina la Mola wako Aliye mkuu. فَسَبِّحْ بِاسْمِ رَبِّكَ الْعَظِيمِ ﴿٧٥﴾

FUNGU 3

76. Basi Ninaapa kwa makundi ya nyota. فَلَآ أُقْسِمُ بِمَوَٰقِعِ النُّجُومِ ﴿٧٦﴾

77. Na hakika hicho bila shaka ni kiapo kikubwa, laiti mngalijua. وَإِنَّهُۥ لَقَسَمٌ لَّوْ تَعْلَمُونَ عَظِيمٌ ﴿٧٧﴾

78. Bila shaka hii ni Kurani yenye heshima, إِنَّهُۥ لَقُرْءَانٌ كَرِيمٌ ﴿٧٨﴾

79. Katika Kitabu kinachohifadhiwa. فِى كِتَٰبٍ مَّكْنُونٍ ﴿٧٩﴾

80. Hawaigusi ila wale waliotakaswa. لَّا يَمَسُّهُۥٓ إِلَّا الْمُطَهَّرُونَ ﴿٨٠﴾

Aya 78, 79 na **80.** Aya hizi zimeeleza sifa tatu za Kurani: (1) *Kurani yenye heshima,* (a) yaani wanaoisoma watakuwa watu wenye kuheshimiwa; (b) mafundisho yake yataheshimiwa. Na ndivyo ilivyo. Leo hii dunia inaheshimu mafundisho ya Kurani iliyoyatoa kukataza kamari, kukataza ulevi, mafundisho ya talaka, ruhusa ya kuoa zaidi ya mke mmoja panapokuwa haja, na mengineyo.

(2) Mafundisho ya Kurani yatahifadhiwa na yatadumu bila kubadilika. (3) (a) Watu waliotakaswa na Allah ndio watakaoifahamu Kurani vizuri (b) mtu akiwa katika hali ya uchafu asishike Kurani. Jambo hili la kutoishika Kurani katika hali ya uchafu limemfanya Rev. J. M.

تَنْزِيْلٌ مِّنْ رَّبِّ الْعٰلَمِيْنَ ﴿٨١﴾

81. Ni uteremsho kutoka kwa Mola wa walimwengu.

اَفَبِهٰذَا الْحَدِيْثِ اَنْتُمْ مُّدْهِنُوْنَ ﴿٨٢﴾

82. Basi je mwayabeza maelezo haya?

وَتَجْعَلُوْنَ رِزْقَكُمْ اَنَّكُمْ تُكَذِّبُوْنَ ﴿٨٣﴾

83. Na mnafanya kuikadhibisha kuwa pato lenu.

فَلَوْلَآ اِذَا بَلَغَتِ الْحُلْقُوْمَ ﴿٨٤﴾

84. Basi mbona (roho) ifikapo kooni,

وَاَنْتُمْ حِيْنَئِذٍ تَنْظُرُوْنَ ﴿٨٥﴾

85. Na ninyi wakati ule mnatazama-

وَنَحْنُ اَقْرَبُ اِلَيْهِ مِنْكُمْ وَلٰكِنْ لَّا تُبْصِرُوْنَ ﴿٨٦﴾

86. Nasi Tunakaribiana nayo zaidi kuliko ninyi, wala ninyi hamwoni-

فَلَوْلَآ اِنْ كُنْتُمْ غَيْرَ مَدِيْنِيْنَ ﴿٨٧﴾

87. Kama ninyi si katika mamlaka ya wengine,

تَرْجِعُوْنَهَآ اِنْ كُنْتُمْ صٰدِقِيْنَ ﴿٨٨﴾

88. Kwa nini hamwirudishi, ikiwa mnasema kweli?

فَاَمَّآ اِنْ كَانَ مِنَ الْمُقَرَّبِيْنَ ﴿٨٩﴾

89. Hivyo akiwa yu miongoni mwa waliokaribishwa,

فَرَوْحٌ وَّرَيْحَانٌ ۙ وَّجَنَّتُ نَعِيْمٍ ﴿٩٠﴾

90. Basi ni raha na manukato na Bustani yenye neema.

وَاَمَّآ اِنْ كَانَ مِنْ اَصْحٰبِ الْيَمِيْنِ ﴿٩١﴾

91. Na kama akiwa yu miongoni mwa watu wa kulia.

فَسَلٰمٌ لَّكَ مِنْ اَصْحٰبِ الْيَمِيْنِ ﴿٩٢﴾

92. Basi ni salama kwako (ewe uliye) miongoni mwa watu wa kulia.

وَاَمَّآ اِنْ كَانَ مِنَ الْمُكَذِّبِيْنَ الضَّآلِّيْنَ ﴿٩٣﴾

93. Na kama akiwa yu miongoni mwa waliokadhibisha, wapotevu,

فَنُزُلٌ مِّنْ حَمِيْمٍ ﴿٩٤﴾

94. Basi karamu yake ni maji yachemkayo.

وَّتَصْلِيَةُ جَحِيْمٍ ﴿٩٥﴾

95. Na kuwaka Motoni.

اِنَّ هٰذَا لَهُوَ حَقُّ الْيَقِيْنِ ﴿٩٦﴾

96. Bila shaka hii ndiyo haki yenye yakini.

فَسَبِّحْ بِاسْمِ رَبِّكَ الْعَظِيْمِ ﴿٩٧﴾ ع ٣ ١٦

97. Basi litukuze jina la Mola wako Mwenye adhama.

Rodwell akiri ya kuwa katika siku za Mtume *s.a.w.* kulikuwa na nakili za Kurani zilizokuwa zinatumiwa na watu sana (The Koran p. 68). Jambo ambalo linazidi kuhakikisha ya kuwa Kurani ilipangwa na Mtume *s.a.w.* mwenyewe siyo na watu wa baadaye kama waelekeavyo kushuku mapadre na wengine.

سُوْرَةُ الْحَدِيْدِ مَدَنِيَّةٌ وَّ هِيَ مَعَ الْبَسْمَلَةِ ثَلَاثُوْنَ اٰيَةً وَّ اَرْبَعَةُ رُكُوْعَاتٍ

57. SURA AL-HADIID

Imeteremshwa Madina

Ina mafungu 4 na Aya 30 pamoja na Bismillahi

بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ ①

1. Kwa jina la Allah, Mwingi wa rehema, Mwingi wa ukarimu.

سَبَّحَ لِلّٰهِ مَا فِي السَّمٰوٰتِ وَالْاَرْضِ ۚ وَهُوَ الْعَزِيْزُ الْحَكِيْمُ ②

2. Kinamtukuza Allah kila kilichomo mbinguni na ardhini, na Yeye ndiye Mwenye ushindi kamili, Mwenye hekima.

لَهٗ مُلْكُ السَّمٰوٰتِ وَالْاَرْضِ ۚ يُحْيٖ وَيُمِيْتُ ۚ وَهُوَ عَلٰى كُلِّ شَيْءٍ قَدِيْرٌ ③

3. Ufalme wa mbingu na ardhi ni Wake; Huhuisha na Hufisha. Na Yeye ni Mwenye uwezo juu ya kila kitu.

هُوَ الْاَوَّلُ وَالْاٰخِرُ وَالظَّاهِرُ وَالْبَاطِنُ ۚ وَهُوَ بِكُلِّ شَيْءٍ عَلِيْمٌ ④

4. Yeye ndiye wa Mwanzo na wa Mwisho, naye ni wa Dhahiri na wa Siri, naye ni Mjuzi wa kila kitu.

هُوَ الَّذِيْ خَلَقَ السَّمٰوٰتِ وَالْاَرْضَ فِيْ سِتَّةِ اَيَّامٍ ثُمَّ اسْتَوٰى عَلَى الْعَرْشِ ؕ يَعْلَمُ مَا يَلِجُ فِي الْاَرْضِ وَمَا يَخْرُجُ مِنْهَا وَمَا يَنْزِلُ مِنَ السَّمَآءِ وَمَا يَعْرُجُ فِيْهَا ؕ وَهُوَ مَعَكُمْ اَيْنَ مَا كُنْتُمْ ؕ وَاللّٰهُ بِمَا تَعْمَلُوْنَ بَصِيْرٌ ⑤

5. Yeye ndiye Aliyeziumba mbingu na ardhi katika nyakati sita: kisha Akastawi katika enzi. Anayajua yanayoingia katika ardhi na yanayotoka humo; na yanayoteremka kutoka mbinguni na yanayopanda humo. Naye Yu pamoja nanyi po pote mlipo. Na Allah Anayaona mnayoyatenda.

لَهٗ مُلْكُ السَّمٰوٰتِ وَالْاَرْضِ ؕ وَاِلَى اللّٰهِ تُرْجَعُ الْاُمُوْرُ ⑥

6. Ufalme wa mbingu na ardhi ni Wake. Na mambo yote hurudishwa kwa Allah.

Sura hii inaitwa *Chuma* kwa mujibu wa adhabu iliyolazimu kupewa makafiri ambao walikusudia kuung'oa Uislamu kwa upanga. Sura hii mpaka sura ya 66 zilishuka Madina (Muhit).

Aya 4. Mtume *s.a.w.* amezieleza Aya hizi nne za Allah namna hii:- "Wewe ni *al-Awwal* (wa Mwanzo) na hakuna cho chote kabla yako. Wewe ni *al-Aakhir* (wa Mwisho) na hakuna cho chote baada yako. Nawe ni *adh-Dhaahir* (Uliye dhahiri) na umeinuka kuliko wote na hakuna kitu juu yako na Wewe ni *al-Baatin* (Mjuzi wa kila kitu) na hakuna kilichofichikana Kwako" (Jami'al Bayan).

يُوْلِجُ الَّيْلَ فِى النَّهَارِ وَيُوْلِجُ النَّهَارَ فِى
الَّيْلِ ؕ وَهُوَ عَلِيْمٌۢ بِذَاتِ الصُّدُوْرِ ۝٧

7. Huuingiza usiku katika mchana na Huuingiza mchana katika usiku. Na Yeye Anayajua yaliyomo vifuani.

اٰمِنُوْا بِاللّٰهِ وَرَسُوْلِهٖ وَاَنْفِقُوْا مِمَّا جَعَلَكُمْ
مُّسْتَخْلَفِيْنَ فِيْهِ ؕ فَالَّذِيْنَ اٰمَنُوْا مِنْكُمْ
وَاَنْفَقُوْا لَهُمْ اَجْرٌ كَبِيْرٌ ۝٨

8. Mwaminini Allah na Mtume Wake, na toeni katika yale Aliyowakabidhini. Basi wale walioamini miongoni mwenu na wakatoa, wana malipo makubwa.

وَمَا لَكُمْ لَا تُؤْمِنُوْنَ بِاللّٰهِ ۚ وَالرَّسُوْلُ
يَدْعُوْكُمْ لِتُؤْمِنُوْا بِرَبِّكُمْ وَقَدْ اَخَذَ
مِيْثَاقَكُمْ اِنْ كُنْتُمْ مُّؤْمِنِيْنَ ۝٩

9. Na mmekuwaje hamumwamini Allah, hali Mtume anawaiteni kumwamini Mola wenu; naye Amekwisha chukua ahadi kwenu, ikiwa ninyi ni waaminio.

هُوَ الَّذِىْ يُنَزِّلُ عَلٰى عَبْدِهٖۤ اٰيٰتٍۢ بَيِّنٰتٍ
لِّيُخْرِجَكُمْ مِّنَ الظُّلُمٰتِ اِلَى النُّوْرِ ؕ
وَاِنَّ اللّٰهَ بِكُمْ لَرَءُوْفٌ رَّحِيْمٌ ۝١٠

10. Yeye Ndiye Anayeteremsha Ishara zilizo wazi juu ya Mtumishi Wake ili kuwatoeni katika giza mwende kwenye nuru, na bila shaka Allah ni Mpole kwenu. Mwenye rehema.

وَمَا لَكُمْ اَلَّا تُنْفِقُوْا فِىْ سَبِيْلِ اللّٰهِ
وَلِلّٰهِ مِيْرَاثُ السَّمٰوٰتِ وَالْاَرْضِ ؕ لَا
يَسْتَوِىْ مِنْكُمْ مَّنْ اَنْفَقَ مِنْ قَبْلِ الْفَتْحِ
وَقٰتَلَ ؕ اُولٰٓئِكَ اَعْظَمُ دَرَجَةً مِّنَ
الَّذِيْنَ اَنْفَقُوْا مِنْۢ بَعْدُ وَقٰتَلُوْا ؕ وَكُلًّا
وَّعَدَ اللّٰهُ الْحُسْنٰى ؕ وَاللّٰهُ بِمَا تَعْمَلُوْنَ
خَبِيْرٌ ۝١١ ع ١١

11. Na mmekuwaje hamtoi katika njia ya Allah na urithi wa mbingu na ardhi ni wa Allah? Hakuna yeyote miongoni mwenu awezaye kuwa sawa na yule aliyetoa na kupigana kabla ya ushindi : hao wana daraja kuu kuliko wale ambao walitoa na kupigana baadae. Na kila mmoja Allah Amemwahidia (ujira mkubwa kabisa), na Allah Anazo habari za yale mnayoyatenda.

FUNGU 2

مَنْ ذَا الَّذِىْ يُقْرِضُ اللّٰهَ قَرْضًا حَسَنًا
فَيُضٰعِفَهٗ لَهٗ وَلَهٗۤ اَجْرٌ كَرِيْمٌ ۝١٢ ۚ

12. Ni nani anayempa Allah karadha nzuri ili Amzidishie? Naye pia ana ujira wenye heshima kubwa.

Aya 12. *Karadha.* Mali au vitu vinavyotolewa katika njia ya Allah vinasemwa hapa kuwa ni karadha anayokopeshwa Allah. Sababu yake ni hii kuwa kitu anachotoa mtu kwa ajili ya Allah ajue kwa yakini kuwa lazima atarudishiwa na atapewa zaidi kuliko alichotoa na pia atapata thawabu kubwa.

يَوْمَ تَرَى الْمُؤْمِنِيْنَ وَالْمُؤْمِنٰتِ يَسْعٰى
نُوْرُهُمْ بَيْنَ اَيْدِيْهِمْ وَبِاَيْمَانِهِمْ
بُشْرٰىكُمُ الْيَوْمَ جَنّٰتٌ تَجْرِيْ مِنْ تَحْتِهَا
الْاَنْهٰرُ خٰلِدِيْنَ فِيْهَا ؕ ذٰلِكَ هُوَ الْفَوْزُ
الْعَظِيْمُ ﴿١٣﴾

13. Siku utakayowaona waaminio wanaume na waaminio wanawake nuru yao ikikimbia kasi mbele yao na upande wao wa kuume (wataambiwa): Furahini leo, ni Bustani zipitazo mito ndani yake, kwa kukaa humo milele, huu ndio ufaulu mkubwa.

يَوْمَ يَقُوْلُ الْمُنٰفِقُوْنَ وَالْمُنٰفِقٰتُ
لِلَّذِيْنَ اٰمَنُوا انْظُرُوْنَا نَقْتَبِسْ مِنْ
نُّوْرِكُمْ ۚ قِيْلَ ارْجِعُوْا وَرَآءَكُمْ
فَالْتَمِسُوْا نُوْرًا ؕ فَضُرِبَ بَيْنَهُمْ
بِسُوْرٍ لَّهٗ بَابٌ ؕ بَاطِنُهٗ فِيْهِ الرَّحْمَةُ
وَظَاهِرُهٗ مِنْ قِبَلِهِ الْعَذَابُ ﴿١٤﴾

14. Siku watakaposema wanafiki wanaume na wanafiki wanawake kuwaambia walioamini: Tungojeeni ili tupate mwangaza katika nuru yenu; Itasemwa: Rudini nyuma yenu na itafuteni nuru. Ndipo ukingo wa ukuta wenye mlango utapigwa kati yao; ndani yake mna rehema na upande wake wa nje kuna adhabu.

يُنَادُوْنَهُمْ اَلَمْ نَكُنْ مَّعَكُمْ ؕ قَالُوْا بَلٰى
وَلٰكِنَّكُمْ فَتَنْتُمْ اَنْفُسَكُمْ وَتَرَبَّصْتُمْ
وَارْتَبْتُمْ وَغَرَّتْكُمُ الْاَمَانِيُّ حَتّٰى جَآءَ
اَمْرُ اللّٰهِ وَغَرَّكُمْ بِاللّٰهِ الْغَرُوْرُ ﴿١٥﴾

15. Watawaita: Je, hatukuwa pamoja nanyi? Watasema: Ndiyo, walakini ninyi mlijitia wenyewe katika fitina na mkangojea na mkaona shaka, na matamanio yakawadanganyeni hata amri ya Allah ikafika, na mdanganyaji amewadanganyeni kwa (habari za) Allah.

فَالْيَوْمَ لَا يُؤْخَذُ مِنْكُمْ فِدْيَةٌ وَّلَا
مِنَ الَّذِيْنَ كَفَرُوْا ؕ مَاْوٰىكُمُ النَّارُ ؕ
هِيَ مَوْلٰىكُمْ ؕ وَبِئْسَ الْمَصِيْرُ ﴿١٦﴾

16. Basi leo haitapokelewa kutoka kwenu fidia wala kutoka kwa wale waliokufuru; makao yenu ni Motoni; ndio rafiki yenu; nayo ni marudio mabaya yaliyoje?

اَلَمْ يَاْنِ لِلَّذِيْنَ اٰمَنُوْٓا اَنْ تَخْشَعَ
قُلُوْبُهُمْ لِذِكْرِ اللّٰهِ وَمَا نَزَلَ مِنَ الْحَقِّ ۙ
وَلَا يَكُوْنُوْا كَالَّذِيْنَ اُوْتُوا الْكِتٰبَ مِنْ
قَبْلُ فَطَالَ عَلَيْهِمُ الْاَمَدُ فَقَسَتْ
قُلُوْبُهُمْ ؕ وَكَثِيْرٌ مِّنْهُمْ فٰسِقُوْنَ ﴿١٧﴾

17. Je, wakati haujafika kwa wale walioamini ya kwamba mioyo yao inyenyekee kwa kumkumbuka Allah na kwa mambo ya haki yaliyoteremka? Wala wasiwe kama wale waliopewa Kitabu zamani na muda wao ukawa mrefu, kwa hiyo mioyo yao ikawa migumu, na wengi wao ni waasi.

Aya 17. Kuonyesha jinsi mafundisho ya Kurani yalivyo na athari juu ya moyo wa mtu, tunatoa hapa tukio moja. Palikuwa na mwizi mmoja mashuhuri sana kwa kwiba. Siku moja usiku alikuwa 37. Na vizazi vingapi Tumeviangamiza kabla yao waliokuwa na nguvu zaidi kuliko hawa, nao waliizunguka miji; je lipo kimbilio?

18. Jueni ya kuwa Allah Huihuisha ardhi baada ya mauti yake; bila shaka Tumewabainishieni Ishara, ili mpate kutumia akili.

اِعْلَمُوْٓا اَنَّ اللّٰهَ يُحْيِ الْاَرْضَ بَعْدَ مَوْتِهَا ؕ قَدْ بَيَّنَّا لَكُمُ الْاٰيٰتِ لَعَلَّكُمْ تَعْقِلُوْنَ ﴿۱۸﴾

19. Kwa hakika wanaume watoao sadaka na wanawake watoao sadaka na wale wanaompa Allah karadha nzuri watazidishiwa maradufu tena watapata malipo mazuri.

اِنَّ الْمُصَّدِّقِيْنَ وَالْمُصَّدِّقٰتِ وَاَقْرَضُوا اللّٰهَ قَرْضًا حَسَنًا يُّضٰعَفُ لَهُمْ وَلَهُمْ اَجْرٌ كَرِيْمٌ ﴿۱۹﴾

20. Na wale waliomwamini Allah na Mitume Wake, hao ndio masiddiki na mashahidi mbele ya Mola wao, watapata malipo yao na nuru yao. Na wale waliokufuru na kukadhibisha Ishara Zetu, hao ndio watu wa Motoni.

وَالَّذِيْنَ اٰمَنُوْا بِاللّٰهِ وَرُسُلِهٖٓ اُولٰٓئِكَ هُمُ الصِّدِّيْقُوْنَ ۖ وَالشُّهَدَآءُ عِنْدَ رَبِّهِمْ ؕ لَهُمْ اَجْرُهُمْ وَنُوْرُهُمْ ؕ وَالَّذِيْنَ كَفَرُوْا وَكَذَّبُوْا بِاٰيٰتِنَآ اُولٰٓئِكَ اَصْحٰبُ الْجَحِيْمِ ﴿۲۰﴾ ع ۲/۱۸

FUNGU 3

21. Jueni ya kwamba maisha ya dunia ni mchezo tu na upuuzi na pambo na kujifaharisha baina yenu, na tamaa ya kuzidiana katika mali na watoto. Mfano wake ni kama mvua ambayo huwafurahisha makafiri maotesho yake, kisha yanakauka na unayaona yenye rangi ya manjano, kisha yanakuwa yenye kuvunjika-vunjika; na katika Akhera kuna adhabu kali na (pia) msamaha wa Allah na radhi (Yake); na maisha ya dunia siyo ila ni starehe idanganyayo.

اِعْلَمُوْٓا اَنَّمَا الْحَيٰوةُ الدُّنْيَا لَعِبٌ وَّلَهْوٌ وَّزِيْنَةٌ وَّتَفَاخُرٌۢ بَيْنَكُمْ وَتَكَاثُرٌ فِى الْاَمْوَالِ وَالْاَوْلَادِ ؕ كَمَثَلِ غَيْثٍ اَعْجَبَ الْكُفَّارَ نَبَاتُهٗ ثُمَّ يَهِيْجُ فَتَرٰىهُ مُصْفَرًّا ثُمَّ يَكُوْنُ حُطَامًا ؕ وَفِى الْاٰخِرَةِ عَذَابٌ شَدِيْدٌ ۙ وَّمَغْفِرَةٌ مِّنَ اللّٰهِ وَرِضْوَانٌ ؕ وَمَا الْحَيٰوةُ الدُّنْيَآ اِلَّا مَتَاعُ الْغُرُوْرِ ﴿۲۱﴾

anasoma Aya hii. Pale pale yule mwizi aliathirika sana moyoni, akarudi na akafanya toba, na leo yeye anajulikana miongoni mwa mawalii wakubwa sana. Jina lake ni Fudhail bin Ayadh (Tadhkira al-Auliya).

Aya 20. Kwa kuwafuata Manabii wa zamani watu waliweza kufikia cheo cha *siddiiq* (ukweli) kuwa ndicho cha juu kabisa. Lakini kwa kumfuata Mtume Muhammad *s.a.w.* ambaye ni mkubwa kuliko Manabii wote na aliyekamilika kabisa, watu wanaweza hata kupewa cheo cha Unabii ambacho ni cheo kikubwa zaidi kuliko cha usiddik (sura 4:70).

سَابِقُوْٓا اِلٰى مَغْفِرَةٍ مِّنْ رَّبِّكُمْ وَجَنَّةٍ
عَرْضُهَا كَعَرْضِ السَّمَآءِ وَالْاَرْضِ ۙ
اُعِدَّتْ لِلَّذِيْنَ اٰمَنُوْا بِاللّٰهِ وَرُسُلِهٖ ؕ
ذٰلِكَ فَضْلُ اللّٰهِ يُؤْتِيْهِ مَنْ يَّشَآءُ ؕ
وَاللّٰهُ ذُو الْفَضْلِ الْعَظِيْمِ ﴿٢٢﴾

22. Shindaneni kuuelekea msamaha wa Mola wenu na kuielekea Pepo ambayo upana wake ni kama upana wa mbingu na ardhi, iliyoandaliwa wale wanao-mwamini Allah na Mitume Wake; hiyo ni fadhili ya Allah, Humpa Amtakaye. Na Allah ni Mwenye fadhili kuu.

مَآ اَصَابَ مِنْ مُّصِيْبَةٍ فِى الْاَرْضِ
وَلَا فِىْٓ اَنْفُسِكُمْ اِلَّا فِىْ كِتٰبٍ مِّنْ قَبْلِ
اَنْ نَّبْرَاَهَا ؕ اِنَّ ذٰلِكَ عَلَى اللّٰهِ يَسِيْرٌ ﴿٢٣﴾

23. Hautokei msiba katika ardhi wala katika nafsi zenu ila huwamo Kitabuni kabla Hatujautoa. Kwa yakini haya ni rahisi kwa Allah.

لِّكَيْلَا تَاْسَوْا عَلٰى مَا فَاتَكُمْ
وَلَا تَفْرَحُوْا بِمَآ اٰتٰىكُمْ ؕ وَاللّٰهُ لَا يُحِبُّ
كُلَّ مُخْتَالٍ فَخُوْرِ ۙ﴿٢٤﴾

24. Ili msihuzunike juu ya kitu kinachowapoteeni wala msijigambe juu ya Anachowapeni. Na Allah Hampendi kila ajivunaye, ajifaharishaye;

الَّذِيْنَ يَبْخَلُوْنَ وَيَاْمُرُوْنَ النَّاسَ
بِالْبُخْلِ ؕ وَمَنْ يَّتَوَلَّ فَاِنَّ اللّٰهَ هُوَ
الْغَنِىُّ الْحَمِيْدُ ﴿٢٥﴾

25. Ambao wanafanya ubahili na kuwaamuru watu wafanye ubahili; na ageukaye, basi hakika Allah ni Mkwasi Asifiwaye.

لَقَدْ اَرْسَلْنَا رُسُلَنَا بِالْبَيِّنٰتِ وَاَنْزَلْنَا
مَعَهُمُ الْكِتٰبَ وَالْمِيْزَانَ لِيَقُوْمَ النَّاسُ
بِالْقِسْطِ ۚ وَاَنْزَلْنَا الْحَدِيْدَ فِيْهِ بَاْسٌ
شَدِيْدٌ وَّمَنَافِعُ لِلنَّاسِ وَلِيَعْلَمَ اللّٰهُ
مَنْ يَّنْصُرُهٗ وَرُسُلَهٗ بِالْغَيْبِ ؕ اِنَّ اللّٰهَ
قَوِىٌّ عَزِيْزٌ ﴿٢٦﴾ ع ١٩

26. Kwa hakika Tuliwapeleka Mitume Wetu kwa dalili waziwazi na Tukakiteremsha pamoja nao Kitabu na mizani, ili watu wasimame kwa uadilifu; na Tukakiteremsha chuma, chenye nguvu nyingi na manufaa kwa watu; na ili Allah Ajulishe wale wanaomsaidia Yeye na Mitume Wake kwa siri. Kwa hakika Allah ni Mwenye nguvu, Mwenye ushindi kamili.

Aya 26. *Tukakiteremsha chuma.* Sio mradi wake kuwa chuma kiliteremka kutoka mbinguni bali maana yake ni kukifanya kiote au kitokee (Razi). Hivyo neno *kuteremsha* au *kushuka* hutumiwa kwa ajili ya kitu chenye manufaa sana kwa watu. Masihi aliyeahidiwa pia imesemwa atashuka, yaani kufika kwake kutakuwa jambo la maana sana. Wala sio mradi wake kuwa atashuka kutoka mbinguni, maana hakuna mahali po pote katika Kurani wala katika Hadithi paliposema kuwa alipanda mbinguni.

Ama chuma kilivyo na maana sana katika kuendesha ustaarabu duniani ni jambo ambalo linaonekana siku hizi zaidi kuliko hapo zamani.

FUNGU 4

وَلَقَدْ اَرْسَلْنَا نُوْحًا وَّ اِبْرٰهِيْمَ وَجَعَلْنَا
فِيْ ذُرِّيَّتِهِمَا النُّبُوَّةَ وَالْكِتٰبَ فَمِنْهُمْ
مُّهْتَدٍ ۚ وَكَثِيْرٌ مِّنْهُمْ فٰسِقُوْنَ ﴿٢٧﴾

27. Na bila shaka Tulimpeleka Nuhu na Ibrahimu na Tukauweka katika wazao wao Unabii na Kitabu; basi wengine wao ni waongofu na wengi wao ni waasi.

ثُمَّ قَفَّيْنَا عَلٰٓى اٰثَارِهِمْ بِرُسُلِنَا
وَقَفَّيْنَا بِعِيْسَى ابْنِ مَرْيَمَ وَاٰتَيْنٰهُ
الْاِنْجِيْلَ ۙ وَجَعَلْنَا فِيْ قُلُوْبِ الَّذِيْنَ
اتَّبَعُوْهُ رَاْفَةً وَّ رَحْمَةً ؕ وَ رَهْبَانِيَّةَ ۨ
ابْتَدَعُوْهَا مَا كَتَبْنٰهَا عَلَيْهِمْ اِلَّا
ابْتِغَآءَ رِضْوَانِ اللّٰهِ فَمَا رَعَوْهَا حَقَّ
رِعَايَتِهَا ۚ فَاٰتَيْنَا الَّذِيْنَ اٰمَنُوْا مِنْهُمْ
اَجْرَهُمْ ۚ وَكَثِيْرٌ مِّنْهُمْ فٰسِقُوْنَ ﴿٢٨﴾

28. Kisha Tukawafuatishia katika nyayo zao Mitume Wetu (wengine) na Tukamfuatisha Isa bin Mariamu na Tukampa Injili; na Tukauweka upole na huruma katika mioyo ya wale waliomfuata; na Sisi Hatukuwafaradhishia uruhubani ule walioubuni wenyewe, ila (Tuliwafaradhishia) wazitafute tu radhi za Allah; lakini hawakutekeleza kama inavyostahili kutekelezwa; basi Tukawapa wale walioamini (na kutenda mema) miongoni mwao ujira wao; na wengi wao walikuwa ni waasi.

يٰٓاَيُّهَا الَّذِيْنَ اٰمَنُوا اتَّقُوا اللّٰهَ وَاٰمِنُوْا
بِرَسُوْلِهٖ يُؤْتِكُمْ كِفْلَيْنِ مِنْ رَّحْمَتِهٖ
وَيَجْعَلْ لَّكُمْ نُوْرًا تَمْشُوْنَ بِهٖ
وَيَغْفِرْ لَكُمْ ؕ وَاللّٰهُ غَفُوْرٌ رَّحِيْمٌ ﴿٢٩﴾

29. Enyi mlioamini, Mcheni Allah na mwaminini Mtume Wake; Atawapeni sehemu mbili za rehema Zake, na Atawafanyieni nuru mtembee kwayo, na Atawaghofirini, na Allah ni Msamehevu, Mrehemevu.

لِّئَلَّا يَعْلَمَ اَهْلُ الْكِتٰبِ اَلَّا يَقْدِرُوْنَ
عَلٰى شَيْءٍ مِّنْ فَضْلِ اللّٰهِ وَ اَنَّ الْفَضْلَ
بِيَدِ اللّٰهِ يُؤْتِيْهِ مَنْ يَّشَآءُ ؕ وَ اللّٰهُ
ذُو الْفَضْلِ الْعَظِيْمِ ﴿٣٠﴾ ع

30. Ili watu wa Kitabu wajue ya kwamba wao hawana uwezo wo wote juu ya fadhili za Allah; na kwa kweli fadhili zimo mikononi mwa Allah, Humpa Amtakaye, na Allah ni Mwenye fadhili kuu.

Aya 28. *Uruhubani* (umonaki) ni desturi ya Wakristo ambao huacha habari za maisha yote ya kidunia na kukaa katika nyumba za watawa, wasiwe na shauri na mambo mengi ya kidunia.

Mtume *s.a.w.* alisema, "Hakuna uruhubani katika Uislamu," Na Kurani inaeleza katika Aya hii ya kuwa desturi hii ya uruhubani Wakristo hawakuamrishwa na Allah bali walijitungia wenyewe, na zaidi ya hayo wasiweze kuitekeleza namna inavyostahili na imewatosa katika maovu ya namna nyingi.

Dini ya Kiislamu inataka Waislamu wanapofanya kazi zao wazifanye vizuri zinavyostahili na wanapofanya ibada na kazi za dini pia wafanye vizuri inavyotakikana. Kuacha mambo ya dunia na kujifunguia chumbani au kukaa porini daima si dini wala si vema.

سُوْرَةُ الْمُجَادَلَةِ مَدَنِيَّةٌ وَّ هِيَ مَعَ الْبَسْمَلَةِ ثَلَاثٌ وَّ عِشْرُوْنَ اٰيَةً وَّ ثَلَاثَةُ رُكُوْعَاتٍ

58. SURA AL-MUJAADILA

Imeteremshwa Madina

Ina mafungu 3 na Aya 23 pamoja na Bismillahi

JUZU 28

بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ ①

1. Kwa jina la Allah, Mwingi wa rehema, Mwingi wa ukarimu.

قَدْ سَمِعَ اللّٰهُ قَوْلَ الَّتِيْ تُجَادِلُكَ فِيْ زَوْجِهَا وَ تَشْتَكِيْۤ اِلَى اللّٰهِ ۖ وَ اللّٰهُ يَسْمَعُ تَحَاوُرَكُمَا ؕ اِنَّ اللّٰهَ سَمِيْعٌۢ بَصِيْرٌ ②

2. Allah Amekwisha sikia kauli ya mwanamke yule aliyejadiliana nawe kuhusiana na mumewe, naye alikuwa akimshtakia Allah wakati Allah alikuwa akiyasikia maongezi yenu wote; hakika Allah ni Asikiaye, Aonaye.

اَلَّذِيْنَ يُظٰهِرُوْنَ مِنْكُمْ مِّنْ نِّسَآئِهِمْ مَّا هُنَّ اُمَّهٰتِهِمْ ؕ اِنْ اُمَّهٰتُهُمْ اِلَّا الّٰٓئِيْ وَلَدْنَهُمْ ؕ وَ اِنَّهُمْ لَيَقُوْلُوْنَ مُنْكَرًا مِّنَ الْقَوْلِ وَ زُوْرًا ؕ وَ اِنَّ اللّٰهَ لَعَفُوٌّ غَفُوْرٌ ③

3. Wale miongoni mwenu wawaitao wake zao mama, wao si mama zao. Mama zao sio ila ni wale waliowazaa. Na kwa yakini hao wanasema maneno mabaya na uwongo; na hakika Allah ni Msamehevu, Mwenye kughofiri.

وَالَّذِيْنَ يُظٰهِرُوْنَ مِنْ نِّسَآئِهِمْ ثُمَّ يَعُوْدُوْنَ لِمَا قَالُوْا فَتَحْرِيْرُ رَقَبَةٍ مِّنْ قَبْلِ اَنْ يَّتَمَآسَّا ؕ ذٰلِكُمْ تُوْعَظُوْنَ بِهٖ ؕ وَ اللّٰهُ بِمَا تَعْمَلُوْنَ خَبِيْرٌ ④

4. Na wale wawaitao wake zao mama, kisha wakarudia katika yale waliyoyasema, basi wampe mtumwa uhuru kabla ya kugusana; hayo ndiyo mnaagizwa kwayo; na Allah Anayajua mnayoyatenda.

Jina la sura hii linatokea katika tukio linaloelezwa katika fungu la kwanza. Ilikuwako desturi ya zamani ya Waarabu ya kutengana na mke kama akimwambia kuwa yu mama yake; haachiki kabisa; haolewi na mtu mwingine, wala hana haki za mke kwa mumewe. Mwislamu mmoja alimwacha mkewe namna hii. Yule mke akanung'unika kwa Mtume *s.a.w.* Desturi hii ilivunjwa na dini ya Kiislamu.

Aya 2. Mwanamke aliyetajwa hapa ni Khaulaa mke wa Aus bin Samit, ambaye mumewe alimwacha kwa mila za zamani za Kiarabu akimwambia: "Wewe kwangu ni kama mgongo wa mama yangu." Kuachana kwa namna hii kunaitwa Dhihaar. Bibi huyu alipeleka habari hii kwa Mtume *s.a.w.* na Mtume akamwambia, Ndiyo amekuacha. Basi bibi yule alishitaki kwa Allah juu ya jambo hili na Allah akateremsha Aya hizi.

فَمَنْ لَّمْ يَجِدْ فَصِيَامُ شَهْرَيْنِ مُتَتَابِعَيْنِ
مِنْ قَبْلِ اَنْ يَّتَمَآسَّا ۚ فَمَنْ لَّمْ يَسْتَطِعْ
فَاِطْعَامُ سِتِّيْنَ مِسْكِيْنًا ؕ ذٰلِكَ
لِتُؤْمِنُوْا بِاللّٰهِ وَرَسُوْلِهٖ ؕ وَتِلْكَ حُدُوْدُ
اللّٰهِ ؕ وَلِلْكٰفِرِيْنَ عَذَابٌ اَلِيْمٌ ۝٥

5. Na asiyepata (mtumwa) basi afunge saumu miezi miwili mfululizo kabla ya kugusana; na asiyeweza, basi awalishe maskini sitini; (mmeambiwa) hayo ili mumwamini Allah na Mtume Wake; na hiyo ni mipaka ya Allah; na kwa makafiri iko adhabu iumizayo.

اِنَّ الَّذِيْنَ يُحَآدُّوْنَ اللّٰهَ وَرَسُوْلَهٗ كُبِتُوْا
كَمَا كُبِتَ الَّذِيْنَ مِنْ قَبْلِهِمْ
وَقَدْ اَنْزَلْنَآ اٰيٰتٍۭ بَيِّنٰتٍ ؕ وَلِلْكٰفِرِيْنَ
عَذَابٌ مُّهِيْنٌ ۚ ۝٦

6. Hakika wale wanaompinza Allah na Mtume Wake watadhalilishwa kama walivyodhalilishwa wale wa kabla yao; na Tumekwisha teremsha Ishara zilizo wazi, na makafiri watapata adhabu ifedheheshayo.

يَوْمَ يَبْعَثُهُمُ اللّٰهُ جَمِيْعًا فَيُنَبِّئُهُمْ بِمَا
عَمِلُوْا ؕ اَحْصٰىهُ اللّٰهُ وَنَسُوْهُ ؕ وَاللّٰهُ عَلٰى
كُلِّ شَيْءٍ شَهِيْدٌ ۝٧ ع

7. Siku Allah Atakayowafufua wote ndipo Atawaambia yale waliyoyatenda: Allah Aliyahesabu nao waliyasahau; na Allah ni Shahidi wa kila kitu.

FUNGU 2

اَلَمْ تَرَ اَنَّ اللّٰهَ يَعْلَمُ مَا فِي السَّمٰوٰتِ وَمَا
فِي الْاَرْضِ ؕ مَا يَكُوْنُ مِنْ نَّجْوٰى ثَلٰثَةٍ
اِلَّا هُوَ رَابِعُهُمْ وَلَا خَمْسَةٍ اِلَّا هُوَ
سَادِسُهُمْ وَلَآ اَدْنٰى مِنْ ذٰلِكَ وَلَآ اَكْثَرَ
اِلَّا هُوَ مَعَهُمْ اَيْنَ مَا كَانُوْا ۚ
ثُمَّ يُنَبِّئُهُمْ بِمَا عَمِلُوْا يَوْمَ الْقِيٰمَةِ ؕ
اِنَّ اللّٰهَ بِكُلِّ شَيْءٍ عَلِيْمٌ ۝٨

8. Je, huoni kwamba Allah Anavijua vilivyomo mbinguni na vilivyomo ardhini? Hawashauriani kwa siri watatu ila Yeye ni wa nne wao, wala watano ila Yeye ni wa sita wao, wala wachache kuliko hao wala zaidi ila Yeye Huwa pamoja nao po pote walipo; kisha siku ya Kiyama Atawaambia waliyoyatenda. Hakika Allah ni Mjuzi wa kila kitu.

اَلَمْ تَرَ اِلَى الَّذِيْنَ نُهُوْا عَنِ النَّجْوٰى
ثُمَّ يَعُوْدُوْنَ لِمَا نُهُوْا عَنْهُ وَيَتَنٰجَوْنَ
بِالْاِثْمِ وَالْعُدْوَانِ وَمَعْصِيَتِ
الرَّسُوْلِ ۫ وَاِذَا جَآءُوْكَ حَيَّوْكَ بِمَا
لَمْ يُحَيِّكَ بِهِ اللّٰهُ ۙ وَيَقُوْلُوْنَ فِيْٓ

9. Je, huwaoni wale waliokatazwa kushauriana kwa siri, kisha wakayarudia waliyokatazwa, na wanashauriana kwa siri juu ya dhambi na uadui na kumwasi Mtume? Na wafikapo kwako wanakuamkia kwa (maamkio) Asiyokuamkia Allah, na

husema katika mioyo yao: Mbona Allah Hatuadhibu kwa haya tuyasemayo? Jahanamu itawatosha; wataiingia, nayo ni mahali pabaya sana pa kurudia.

اَنْفُسِهِمْ لَوْلَا يُعَذِّبُنَا اللّٰهُ بِمَا نَقُوْلُ ؕ حَسْبُهُمْ جَهَنَّمُ ۚ يَصْلَوْنَهَا ۚ فَبِئْسَ الْمَصِيْرُ ۝٨

10. Enyi mlioamini! mnaposhauriana kwa siri, basi msishauriane juu ya dhambi na uadui na kumwasi Mtume, bali shaurianeni juu ya wema na utawa; na mcheni Allah Ambaye Kwake mtakusanywa.

يٰۤاَيُّهَا الَّذِيْنَ اٰمَنُوْۤا اِذَا تَنَاجَيْتُمْ فَلَا تَتَنَاجَوْا بِالْاِثْمِ وَالْعُدْوَانِ وَمَعْصِيَتِ الرَّسُوْلِ وَتَنَاجَوْا بِالْبِرِّ وَالتَّقْوٰى ؕ وَاتَّقُوا اللّٰهَ الَّذِيْۤ اِلَيْهِ تُحْشَرُوْنَ ۝١٠

11. Kwa yakini kushauriana kwa siri kunatokana na Shetani ili awahuzunishe wale walioamini, lakini hawezi kuwadhuru cho chote ila kwa idhini ya Allah; na waaminio, basi wamtegemee Allah tu.

اِنَّمَا النَّجْوٰى مِنَ الشَّيْطٰنِ لِيَحْزُنَ الَّذِيْنَ اٰمَنُوْا وَلَيْسَ بِضَآرِّهِمْ شَيْـًٔا اِلَّا بِاِذْنِ اللّٰهِ ؕ وَعَلَى اللّٰهِ فَلْيَتَوَكَّلِ الْمُؤْمِنُوْنَ ۝١١

12. Enyi mlioamini! mnapoambiwa: Fanyeni nafasi katika mikutano, basi fanyeni nafasi, Allah Atawafanyieni nafasi. Na inaposemwa simameni, basi simameni. Allah Atawanyanyua wale walioamini miongoni mwenu na waliopewa elimu katika madaraja; na Allah Anazo habari za mnayoyatenda.

يٰۤاَيُّهَا الَّذِيْنَ اٰمَنُوْۤا اِذَا قِيْلَ لَكُمْ تَفَسَّحُوْا فِى الْمَجٰلِسِ فَافْسَحُوْا يَفْسَحِ اللّٰهُ لَكُمْ ۚ وَاِذَا قِيْلَ انْشُزُوْا فَانْشُزُوْا يَرْفَعِ اللّٰهُ الَّذِيْنَ اٰمَنُوْا مِنْكُمْ ۙ وَالَّذِيْنَ اُوْتُوا الْعِلْمَ دَرَجٰتٍ ؕ وَاللّٰهُ بِمَا تَعْمَلُوْنَ خَبِيْرٌ ۝١٢

13. Enyi mlioamini! mnapotaka kushauriana (jambo binafsi) na Mtume faraghani, basi tangulizeni sadaka kabla ya kushauriana kwenu; hilo ni jambo bora kwenu na lililotakasika zaidi. Ikiwa hamkupata (cha kutoa), basi bila shaka Allah ni Msamehevu, Mrehemevu.

يٰۤاَيُّهَا الَّذِيْنَ اٰمَنُوْۤا اِذَا نَاجَيْتُمُ الرَّسُوْلَ فَقَدِّمُوْا بَيْنَ يَدَىْ نَجْوٰىكُمْ صَدَقَةً ؕ ذٰلِكَ خَيْرٌ لَّكُمْ وَاَطْهَرُ ؕ فَاِنْ لَّمْ تَجِدُوْا فَاِنَّ اللّٰهَ غَفُوْرٌ رَّحِيْمٌ ۝١٣

Aya 10. Islam anakataza mkutano wa siri unaoshauriana juu ya mambo ya uasi na kuvunja sheria. Waislamu hawana ruhusa kuingia vyama na mikutano ya namna hii. Mikutano iliyoruhusiwa ni ile inayotajwa katika sura 4:115.

Aya 12. *Inaposemwa, Simameni, basi simameni.* Hizi ndizo adabu za mikutano zinazoelezwa katika Aya hizi: Mtu akiambiwa asimame au atoe nafasi, basi afanye tu, maana Allah anasema, jambo hili halimteremshi cheo mtu aliyeamini, bali Allah *atawarufaisha* wale walioamini. Neno hili *kurufaishwa* lililotumiwa kwa ajili ya waaminio linaweza kuwaongoza wale wanaodhani kuwa kurufaishwa kwa Nabii Isa ni kupelekwa mbinguni, kwani

ءَ اَشْفَقْتُمْ اَنْ تُقَدِّمُوْا بَيْنَ يَدَىْ
نَجْوٰىكُمْ صَدَقٰتٍ ؕ فَاِذْ لَمْ تَفْعَلُوْا
وَ تَابَ اللّٰهُ عَلَيْكُمْ فَاَقِيْمُوا الصَّلٰوةَ
وَاٰتُوا الزَّكٰوةَ وَ اَطِيْعُوا اللّٰهَ وَرَسُوْلَهٗ ؕ
وَاللّٰهُ خَبِيْرٌۢ بِمَا تَعْمَلُوْنَ ﴿۱۴﴾ ع ۲/۴

14. Je, ninyi mnaogopa kuzitanguliza sadaka kabla ya mashauriano yenu (binafsi)? Lakini kama hamuwezi kufanya hivyo, wakati Allah Ameshaikubali toba yenu, basi msimamishe Sala na mtoe zaka na muwatii Allah na Mtume wake. Na Allah daima Ana habari ya yale mnayoyatenda.

FUNGU 3

اَلَمْ تَرَ اِلَى الَّذِيْنَ تَوَلَّوْا قَوْمًا غَضِبَ
اللّٰهُ عَلَيْهِمْ ؕ مَا هُمْ مِّنْكُمْ وَلَا مِنْهُمْ ۙ
وَ يَحْلِفُوْنَ عَلَى الْكَذِبِ وَهُمْ
يَعْلَمُوْنَ ﴿۱۵﴾

15. Je, hukuwaona wale waliofanya urafiki na watu aliowakasirikia Allah? Hao si miongoni mwenu wala si miongoni mwao, na huapa kwa uwongo hali wanajua.

اَعَدَّ اللّٰهُ لَهُمْ عَذَابًا شَدِيْدًا ؕ اِنَّهُمْ سَآءَ
مَا كَانُوْا يَعْمَلُوْنَ ﴿۱۶﴾

16. Allah Amewaandalia adhabu kali; kwa hakika waliyokuwa wakiyatenda ni mabaya.

اِتَّخَذُوْۤا اَيْمَانَهُمْ جُنَّةً فَصَدُّوْا عَنْ
سَبِيْلِ اللّٰهِ فَلَهُمْ عَذَابٌ مُّهِيْنٌ ﴿۱۷﴾

17. Wamefanya kiapo chao kuwa ngao wakaepuka njia ya Allah; basi itakuwa kwao adhabu ifedheheshayo.

لَنْ تُغْنِىَ عَنْهُمْ اَمْوَالُهُمْ وَ لَاۤ
اَوْلَادُهُمْ مِّنَ اللّٰهِ شَيْـًٔا ؕ اُولٰٓئِكَ اَصْحٰبُ
النَّارِ ؕ هُمْ فِيْهَا خٰلِدُوْنَ ﴿۱۸﴾

18. Mali zao na watoto wao havitawafaa kitu mbele ya Allah; hao ndio watu wa Motoni, humo watakaa.

يَوْمَ يَبْعَثُهُمُ اللّٰهُ جَمِيْعًا فَيَحْلِفُوْنَ لَهٗ
كَمَا يَحْلِفُوْنَ لَكُمْ وَ يَحْسَبُوْنَ اَنَّهُمْ
عَلٰى شَىْءٍ ؕ اَلَاۤ اِنَّهُمْ هُمُ الْكٰذِبُوْنَ ﴿۱۹﴾

19. Siku Allah Atakapowafufua wote ndipo wataapa mbele Yake kama wanavyoapa mbele yenu, na watadhani ya kwamba wana kitu. Tahadharini! Kwa hakika hao ndio waongo.

اِسْتَحْوَذَ عَلَيْهِمُ الشَّيْطٰنُ فَاَنْسٰىهُمْ ذِكْرَ
اللّٰهِ ؕ اُولٰٓئِكَ حِزْبُ الشَّيْطٰنِ ؕ اَلَاۤ اِنَّ
حِزْبَ الشَّيْطٰنِ هُمُ الْخٰسِرُوْنَ ﴿۲۰﴾

20. Shetani amewatawala, kwa hivyo akawasahaulisha kumkumbuka Allah. Hao ndio kundi la Shetani. Sikilizeni! kwa hakika kundi la Shetani ndio wenye hasara.

tena itakuwa hata waaminio warufaishwao hupelekwa mbinguni, nayo sivyo. Neno hili maana yake ni kunyanyua daraja na cheo.

21. Kwa yakini wale wanaompinza Allah na Mtume Wake, hao ndio miongoni mwa waliodhalilika.

إِنَّ الَّذِيْنَ يُحَآدُّوْنَ اللّٰهَ وَرَسُوْلَهٗٓ
أُولٰٓئِكَ فِي الْأَذَلِّيْنَ ﴿٢١﴾

22. Allah Amekwisha andika: Bila shaka Nitashinda Mimi na Mitume Wangu! Hakika Allah ni Mwenye nguvu, Mwenye ushindi kamili.

كَتَبَ اللّٰهُ لَأَغْلِبَنَّ أَنَا وَرُسُلِيْ ۚ إِنَّ اللّٰهَ
قَوِيٌّ عَزِيْزٌ ﴿٢٢﴾

23. Hutapata watu wanaomwamini Allah na siku ya Mwisho kuwapenda wale wanaompinza Allah na Mtume Wake, lau kama ni baba zao au watoto wao au ndugu zao au jamaa zao. Hao ndio Ameiandika mioyoni mwao imani na Akawasaidia kwa Roho itokayo Kwake: Na Atawaingiza katika Mabustani yapitayo mito ndani yao, humo watakaa. Allah Amekuwa radhi nao, na wao wamekuwa radhi Naye; hao ndio kundi la Allah. Sikilizeni! Hakika kundi la Allah ndio wanaofaulu.

لَا تَجِدُ قَوْمًا يُّؤْمِنُوْنَ بِاللّٰهِ وَالْيَوْمِ
الْآخِرِ يُوَآدُّوْنَ مَنْ حَآدَّ اللّٰهَ وَرَسُوْلَهٗ
وَلَوْ كَانُوْٓا اٰبَآءَهُمْ أَوْ أَبْنَآءَهُمْ أَوْ
إِخْوَانَهُمْ أَوْ عَشِيْرَتَهُمْ ۚ أُولٰٓئِكَ كَتَبَ
فِيْ قُلُوْبِهِمُ الْإِيْمَانَ وَأَيَّدَهُمْ بِرُوْحٍ
مِّنْهُ ۖ وَيُدْخِلُهُمْ جَنّٰتٍ تَجْرِيْ مِنْ
تَحْتِهَا الْأَنْهٰرُ خٰلِدِيْنَ فِيْهَا ۚ رَضِيَ اللّٰهُ
عَنْهُمْ وَرَضُوْا عَنْهُ ۚ أُولٰٓئِكَ حِزْبُ اللّٰهِ ۚ
أَلَآ إِنَّ حِزْبَ اللّٰهِ هُمُ الْمُفْلِحُوْنَ ﴿٢٣﴾ ع

Aya 22. Mungu amekwisha weka kanuni ya kuwa Yeye na Mitume Wake watashinda. Na kweli, wakashinda, hali habari imetolewa mbele. Mambo haya yanadhihirisha kuwa Mungu yupo. Lakini Wakristo wanafikiri Yesu ni mwana wa Mungu, naye akashindwa na watu na akafikishwa msalabani! Siyo jambo la ajabu? Kwa mujibu wa itikadi yao inaonekana ya kuwa Yesu hakupewa hata heshima inayopewa Manabii wengine. Sisi tunajua Yesu alikuwa Nabii tu na hakufishwa msalabani bali alishinda kama wanavyoshinda Manabii wa Allah.

Aya 23. *Akawasaidia kwa Roho itokayo Kwake,* yaani masahaba wa Mtume *s.a.w.* walisaidiwa na roho itokayo kwa Allah kama vile alivyosaidiwa Yesu. Sasa Wakristo wanaochukua uungu kwa maneno namna hii watasimama wapi? Kwa mujibu wa Aya hii msaada alopewa Yesu wa Roho ni sawa na ule waliopewa masahaba wa Mtume *s.a.w.* Ama kwa cheo, Mtume *s.a.w.* amewapita Manabii wengine wote, hata akasema: "Kama Musa na Isa wangekuwa hai wasingekuwa na njia ila kunifuata" (Hashiya Ibn Kathir, jalada 2: Alyawakit waljawahiri, jalada 2).

Masahaba wamesaidiwa kwa *Roho iliyotoka Kwake*. Roho huyo ni Mtume *s.a.w.* Hapa Wakristo wanakumbushwa bishara iliyomo katika Yohana 16:13 ya kwamba yule Roho wa Kweli amekwisha fika naye ni Mtume Muhammad *s.a.w.* naye amewasaidia waaminio.

سُوْرَةُ الْحَشْرِ مَدَنِيَّةٌ وَّ هِيَ مَعَ الْبَسْمَلَةِ خَمْسٌ وَّ عِشْرُوْنَ اٰيَةً وَّ ثَلَاثَةُ رُكُوْعَاتٍ

59. SURA AL-HASHR

Imeteremshwa Madina

Ina mafungu 3 na Aya 25 pamoja na Bismillahi

بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ ①

1. Kwa jina la Allah, Mwingi wa rehema, Mwingi wa ukarimu.

سَبَّحَ لِلّٰهِ مَا فِي السَّمٰوٰتِ وَمَا فِي الْاَرْضِ ۚ وَهُوَ الْعَزِيْزُ الْحَكِيْمُ ②

2. Vinamtukuza Allah vilivyomo mbinguni na vilivyomo ardhini, na Yeye ni Mwenye nguvu, Mwenye hekima.

هُوَ الَّذِيْٓ اَخْرَجَ الَّذِيْنَ كَفَرُوْا مِنْ اَهْلِ الْكِتٰبِ مِنْ دِيَارِهِمْ لِاَوَّلِ الْحَشْرِ ؕ مَا ظَنَنْتُمْ اَنْ يَّخْرُجُوْا وَظَنُّوْٓا اَنَّهُمْ مَّانِعَتُهُمْ حُصُوْنُهُمْ مِّنَ اللّٰهِ فَاَتٰىهُمُ اللّٰهُ مِنْ حَيْثُ لَمْ يَحْتَسِبُوْا ۗ وَقَذَفَ فِيْ قُلُوْبِهِمُ الرُّعْبَ يُخْرِبُوْنَ بُيُوْتَهُمْ بِاَيْدِيْهِمْ وَاَيْدِي الْمُؤْمِنِيْنَ ۗ فَاعْتَبِرُوْا يٰٓاُولِي الْاَبْصَارِ ③

3. Yeye ndiye Aliyewatoa waliokufuru miongoni mwa watu wa Kitabu katika nyumba zao wakati wa uhamisho wa kwanza; hamkudhani ya kuwa watatoka, nao walidhani ya kuwa ngome zao zitawalinda na Allah; lakini Allah Akawafikia kwa mahali wasipopatazamia, na Akatia woga katika mioyo yao; wakazivunja nyumba zao kwa mikono yao na kwa mikono ya waaminio; basi pateni somo, enyi wenye busara!

وَلَوْلَآ اَنْ كَتَبَ اللّٰهُ عَلَيْهِمُ الْجَلَآءَ لَعَذَّبَهُمْ فِي الدُّنْيَا ۭ وَلَهُمْ فِي الْاٰخِرَةِ عَذَابُ النَّارِ ④

4. Na lau kama Allah Asingaliwaandikia kufukuzwa Angaliwa-adhibu duniani, na katika Akhera watapata adhabu ya Moto.

ذٰلِكَ بِاَنَّهُمْ شَاۗقُّوا اللّٰهَ وَرَسُوْلَهٗ ۚ وَمَنْ يُّشَاۗقِّ اللّٰهَ فَاِنَّ اللّٰهَ شَدِيْدُ الْعِقَابِ ⑤

5. Hayo ni kwa sababu walimhalifu Allah na Mtume Wake, na anayemhalifu Allah basi kwa hakika Allah ni Mkali wa kuadhibu.

Sura hii inaitwa *Kufukuza* kwa sababu inaeleza habari za kufukuzwa kabila la Kiyahudi lililoitwa Banu Nadhir. Hapana shaka sura hii ilishuka Madina muda kidogo baada ya kufukuzwa hao Mayahudi.

Aya 3. *Uhamisho wa kwanza.* Uhamisho uliotajwa hapa ni ule waliohamishwa Mayahudi wa kabila la Banu Nadhir wa Madina miezi sita baada ya vita vya Uhud. Mayahudi hawa walifanya

مَا قَطَعْتُمْ مِّنْ لِّيْنَةٍ اَوْ تَرَكْتُمُوْهَا
قَآئِمَةً عَلٰٓى اُصُوْلِهَا فَبِاِذْنِ اللّٰهِ
وَلِيُخْزِيَ الْفٰسِقِيْنَ ۝٦

6. Mtende wo wote mlioukata au mliouacha ukisimama kwa mizizi yake, basi ni kwa idhini ya Allah, na kuwafedhehesha wavunjao sheria.

وَمَآ اَفَآءَ اللّٰهُ عَلٰى رَسُوْلِهٖ مِنْهُمْ فَمَآ
اَوْجَفْتُمْ عَلَيْهِ مِنْ خَيْلٍ وَّلَا رِكَابٍ
وَّلٰكِنَّ اللّٰهَ يُسَلِّطُ رُسُلَهٗ عَلٰى مَنْ يَّشَآءُ ؕ
وَاللّٰهُ عَلٰى كُلِّ شَيْءٍ قَدِيْرٌ ۝٧

7. Na mali Aliyoileta Allah kwa Mtume Wake kutoka kwao hamkuiendea kwa farasi wala kwa ngamia, lakini Allah Huwapa mamlaka Mitume Wake juu ya ye yote Amtakaye; na Allah ni Mwenye uwezo juu ya kila kitu.

مَآ اَفَآءَ اللّٰهُ عَلٰى رَسُوْلِهٖ مِنْ اَهْلِ الْقُرٰى
فَلِلّٰهِ وَلِلرَّسُوْلِ وَلِذِي الْقُرْبٰى وَالْيَتٰمٰى
وَالْمَسٰكِيْنِ وَابْنِ السَّبِيْلِ ۙ كَيْ لَا يَكُوْنَ
دُوْلَةً ۢ بَيْنَ الْاَغْنِيَآءِ مِنْكُمْ ؕ وَمَآ اٰتٰىكُمُ
الرَّسُوْلُ فَخُذُوْهُ ۗ وَمَا نَهٰىكُمْ عَنْهُ
فَانْتَهُوْا ۚ وَاتَّقُوا اللّٰهَ ؕ اِنَّ اللّٰهَ شَدِيْدُ
الْعِقَابِ ۝٨

8. Mali Aliyoileta Allah kwa Mtume Wake kutoka kwa watu wa vijijini ni kwa ajili ya Allah, na Mtume, na jamaa wa karibu na mayatima na maskini na wasafiri; ili isiwe inayorudia baina ya matajiri wenu tu. Na anachowapeni Mtume basi pokeeni, na anachowakatazeni basi jiepusheni; na Mwogopeni Allah; kwa yakini Allah ni Mkali wa kuadhibu.

لِلْفُقَرَآءِ الْمُهٰجِرِيْنَ الَّذِيْنَ اُخْرِجُوْا
مِنْ دِيَارِهِمْ وَاَمْوَالِهِمْ يَبْتَغُوْنَ فَضْلًا
مِّنَ اللّٰهِ وَرِضْوَانًا وَّيَنْصُرُوْنَ اللّٰهَ
وَرَسُوْلَهٗ ؕ اُولٰٓئِكَ هُمُ الصّٰدِقُوْنَ ۝٩

9. (Na mali hiyo) ni kwa mafukara waliohama ambao walifukuzwa katika nyumba zao na mali zao wakizitafuta fadhili za Allah na radhi (Zake), na wanamsaidia Allah na Mtume Wake. Hao ndio wakweli.

---

hiyana na uasi na kuvunja mapatano ambayo kwa mujibu wa kanuni ingestahili wauwawe. Lakini Mtume *s.a.w.* aliwahurumia na akawahamisha tu.

Aya 8. *Ili isiwe inayorudia baina ya matajiri wenu tu.* Dini ya Kiislamu imeangalia sana habari za mgawanyiko wa mali ili ipate kuenea sana kati ya watu na isijikusanye katika mikono ya matajiri wachache na maskini wakabaki wanalemewa na umaskini wao.

وَالَّذِيْنَ تَبَوَّؤُ الدَّارَ وَالْاِيْمَانَ مِنْ
قَبْلِهِمْ يُحِبُّوْنَ مَنْ هَاجَرَ اِلَيْهِمْ وَلَا
يَجِدُوْنَ فِيْ صُدُوْرِهِمْ حَاجَةً مِّمَّآ
اُوْتُوْا وَيُؤْثِرُوْنَ عَلٰٓى اَنْفُسِهِمْ وَلَوْ كَانَ
بِهِمْ خَصَاصَةٌ ۭ وَمَنْ يُّوْقَ شُحَّ نَفْسِهٖ
فَاُولٰۗىِٕكَ هُمُ الْمُفْلِحُوْنَ ۝

10. Na (pia kwa) wale waliokwisha andaa nyumba kabla yao na kuwa na imani mioyoni, wanawapenda waliohamia kwao, wala hawapati dhiki mioyoni mwao kwa hayo waliyopewa, (wahamao), na wanawapendelea wengine kuliko nafsi zao ingawa wenyewe wana hali ndogo. Na aepushwaye na ubahili wa nafsi yake, basi hao ndio wenye kufaulu.

وَالَّذِيْنَ جَاۗءُوْ مِنْۢ بَعْدِهِمْ يَقُوْلُوْنَ رَبَّنَا
اغْفِرْ لَنَا وَلِاِخْوَانِنَا الَّذِيْنَ سَبَقُوْنَا
بِالْاِيْمَانِ وَلَا تَجْعَلْ فِيْ قُلُوْبِنَا غِلًّا
لِّلَّذِيْنَ اٰمَنُوْا رَبَّنَآ اِنَّكَ رَءُوْفٌ رَّحِيْمٌ ۝

11. Na waliofika baada yao wanasema: Mola wetu, Utughofiri pamoja na ndugu zetu waliotutangulia katika imani wala Usiweke mfundo katika mioyo yetu kwa walioamini; Mola wetu, hakika Wewe ni Mpole sana, Mwingi wa Ukarimu.

FUNGU 2

اَلَمْ تَرَ اِلَى الَّذِيْنَ نَافَقُوْا يَقُوْلُوْنَ
لِاِخْوَانِهِمُ الَّذِيْنَ كَفَرُوْا مِنْ
اَهْلِ الْكِتٰبِ لَىِٕنْ اُخْرِجْتُمْ لَنَخْرُجَنَّ
مَعَكُمْ وَلَا نُطِيْعُ فِيْكُمْ اَحَدًا اَبَدًا ۙ
وَّاِنْ قُوْتِلْتُمْ لَنَنْصُرَنَّكُمْ ۭ وَاللّٰهُ يَشْهَدُ
اِنَّهُمْ لَكٰذِبُوْنَ ۝

12. Je, hukuwaona wale waliofanya unafiki wanawaambia ndugu zao waliokufuru miongoni mwa watu wa Kitabu: Kama mkifukuzwa bila shaka nasi pia tutaondoka pamoja nanyi, wala hatutamtii ye yote kabisa juu yenu; na kama mkipigwa vita lazima tutawasaidieni; na Allah Anashuhudia ya kuwa wao kwa hakika ni waongo hasa.

Aya 10. *Walioahamia kwao* ni Waislamu waliotoka Makka na kuhamia Madina, na wakaitwa *Muhaajiriin,* yaani *waliohama.* Na Waislamu wenyeji wa Madina wakaitwa *Ansaar* yaani *wasaidizi.*

Wanawapendelea kuliko nafsi zao. Ansaar walifanya kila namna ya bidii ili kuwastarehesha ndugu zao waliohamia kwao. Hata wengine waliokuwa na wake wawili wawili waliacha mmoja mmoja ili waolewe na ndugu zao waliotoka Makka. Huu ndio udugu wa ajabu uliosimamishwa na Mtume *s.a.w.* (Baidhawi).

Ingawa wenyewe wana hali ndogo. Siku moja alifika Madina Mwislamu aliyekuwa amehama kutoka Makka, naye ana njaa. Mtume *s.a.w.* akauliza msikitini nani atamkaribisha mgeni yule. Ansar mmoja akasema, Mimi; na akamchukua mpaka nyumbani kwake, na akamwambia mkewe, mlishe vizuri mgeni huyu ni wa Mtume *s.a.w.* Mkewe akamjibu, nyumbani hamna chakula isipokuwa kidogo kwa ajili ya watoto. Basi akashauriana na mkewe awalaze watoto mapema, na asiwashe taa, kisha alete chakula wampe mgeni gizani ili naye akae karibu naye ajifanye kama anakula kwa kutafuna kinywa kitupu. Kwa njia hii wakamlisha mgeni hata akashiba na wenyewe wakalala na njaa hali mgeni hana habari.

13. Kama wakifukuzwa hawatatoka pamoja nao, na kama wakipigwa hawatawasaidia, na kama wakiwasaidia kwa yakini watageuza migongo, kisha hawatasaidiwa.

لَئِنْ اُخْرِجُوْا لَا يَخْرُجُوْنَ مَعَهُمْ ۚ وَلَئِنْ قُوْتِلُوْا لَا يَنْصُرُوْنَهُمْ ۚ وَلَئِنْ نَّصَرُوْهُمْ لَيُوَلُّنَّ الْاَدْبَارَ ۫ ثُمَّ لَا يُنْصَرُوْنَ ﴿١٣﴾

14. Hakika ninyi mnaogopwa zaidi katika mioyo yao kuliko Allah; hayo ni kwa sababu wao ni watu wasiofahamu.

لَاَنْتُمْ اَشَدُّ رَهْبَةً فِيْ صُدُوْرِهِمْ مِّنَ اللّٰهِ ؕ ذٰلِكَ بِاَنَّهُمْ قَوْمٌ لَّا يَفْقَهُوْنَ ﴿١٤﴾

15. Hawatapigana nanyi kwa umoja wao isipokuwa katika vijiji vilivyohifadhiwa, au nyuma ya kuta; mapigano yao baina yao ni makali; unawadhani kuwa wao ni wamoja wakati mioyo yao imefarakana. Hayo ni kwa sababu wao ni watu wasio na akili.

لَا يُقَاتِلُوْنَكُمْ جَمِيْعًا اِلَّا فِيْ قُرًى مُّحَصَّنَةٍ اَوْ مِنْ وَّرَآءِ جُدُرٍ ؕ بَاْسُهُمْ بَيْنَهُمْ شَدِيْدٌ ؕ تَحْسَبُهُمْ جَمِيْعًا وَّقُلُوْبُهُمْ شَتّٰى ؕ ذٰلِكَ بِاَنَّهُمْ قَوْمٌ لَّا يَعْقِلُوْنَ ﴿١٥﴾

16. (Hali yao ni) kama ya wale waliowatangulia hivi karibuni; walionja ubaya wa mambo yao, nao watapata adhabu iumizayo.

كَمَثَلِ الَّذِيْنَ مِنْ قَبْلِهِمْ قَرِيْبًا ذَاقُوْا وَبَالَ اَمْرِهِمْ ۚ وَلَهُمْ عَذَابٌ اَلِيْمٌ ﴿١٦﴾

17. Ni kama Shetani alipomwambia mtu: Kufuru; lakini alipokufuru, akasema: Mimi si pamoja nawe; hakika namwogopa Allah, Mola wa walimwengu.

كَمَثَلِ الشَّيْطٰنِ اِذْ قَالَ لِلْاِنْسَانِ اكْفُرْ ۚ فَلَمَّا كَفَرَ قَالَ اِنِّيْ بَرِيْٓءٌ مِّنْكَ اِنِّيْٓ اَخَافُ اللّٰهَ رَبَّ الْعٰلَمِيْنَ ﴿١٧﴾

18. Basi mwisho wa wote wawili ukawa kwamba waingie Motoni kukaa humo; na huo ndio ujira wa wadhalimu.

فَكَانَ عَاقِبَتَهُمَآ اَنَّهُمَا فِي النَّارِ خَالِدَيْنِ فِيْهَا ؕ وَذٰلِكَ جَزٰٓؤُا الظّٰلِمِيْنَ ﴿١٨﴾ ع

FUNGU 3

19. Enyi mlioamini! Mcheni Allah, na kila nafsi iangalie ilichotanguliza kwa ajili ya kesho, na

يٰٓاَيُّهَا الَّذِيْنَ اٰمَنُوا اتَّقُوا اللّٰهَ وَلْتَنْظُرْ نَفْسٌ مَّا قَدَّمَتْ لِغَدٍ ۚ وَاتَّقُوا اللّٰهَ ؕ

Allah alimfahamisha Mtume *s.a.w.* jambo hili, na asubuhi Mtume akamwambia sahaba yule, Ulifanya nini jana usiku. Allah alifurahi sana kwa akili uliyopitisha. (Bukhari).

Aya 19. Aya hii husomwa katika sehemu ya tatu ya hotuba ya Nikaha (ndoa).

اِنَّ اللّٰهَ خَبِيْرٌۢ بِمَا تَعْمَلُوْنَ ﴿١٩﴾

mcheni Allah; hakika Allah Anazo habari za mnayoyatenda.

وَلَا تَكُوْنُوْا كَالَّذِيْنَ نَسُوا اللّٰهَ فَاَنْسٰىهُمْ اَنْفُسَهُمْ ؕ اُولٰٓئِكَ هُمُ الْفٰسِقُوْنَ ﴿٢٠﴾

20. Wala msiwe kama wale waliomsahau Allah, kwa hiyo Akawasahaulisha nafsi zao. Hao ndio wavunjao sheria.

لَا يَسْتَوِيْٓ اَصْحٰبُ النَّارِ وَاَصْحٰبُ الْجَنَّةِ ؕ اَصْحٰبُ الْجَنَّةِ هُمُ الْفَآئِزُوْنَ ﴿٢٠﴾

21. Hawawi sawa watu wa Motoni na watu wa Peponi; watu wa Peponi ndio wenye kufuzu.

لَوْ اَنْزَلْنَا هٰذَا الْقُرْاٰنَ عَلٰى جَبَلٍ لَّرَاَيْتَهٗ خَاشِعًا مُّتَصَدِّعًا مِّنْ خَشْيَةِ اللّٰهِ ؕ وَتِلْكَ الْاَمْثَالُ نَضْرِبُهَا لِلنَّاسِ لَعَلَّهُمْ يَتَفَكَّرُوْنَ ﴿٢١﴾

22. Lau kama Tungaliiteremsha hii Kurani juu ya mlima, ungaliuona ukinyenyekea (na) kupasuka kwa sababu ya hofu ya Allah; na hizi ni methali Tunazowaeleza watu ili watafakari.

هُوَ اللّٰهُ الَّذِيْ لَآ اِلٰهَ اِلَّا هُوَ ۚ عٰلِمُ الْغَيْبِ وَالشَّهَادَةِ ۚ هُوَ الرَّحْمٰنُ الرَّحِيْمُ ﴿٢٢﴾

23. Yeye Ndiye Allah Ambaye hapana apasaye kuabudiwa isipokuwa Yeye; Ajuaye yasiyoonekana na yanayoonekana; Yeye ndiye Mwingi wa rehema, Mwingi wa ukarimu.

هُوَ اللّٰهُ الَّذِيْ لَآ اِلٰهَ اِلَّا هُوَ ۚ اَلْمَلِكُ الْقُدُّوْسُ السَّلٰمُ الْمُؤْمِنُ الْمُهَيْمِنُ الْعَزِيْزُ الْجَبَّارُ الْمُتَكَبِّرُ ؕ سُبْحٰنَ اللّٰهِ عَمَّا يُشْرِكُوْنَ ﴿٢٣﴾

24. Yeye Ndiye Allah, Ambaye hapana apasaye kuabudiwa isipokuwa Yeye; Mfalme, Mtakatifu, Mwenye salama, Mtoaji wa amani, Mwangaliaji, Mwenye shani, Jabbari, Mkubwa. Allah Yu mbali na hao wanaomshirikisha Naye.

هُوَ اللّٰهُ الْخَالِقُ الْبَارِئُ الْمُصَوِّرُ لَهُ الْاَسْمَآءُ الْحُسْنٰى ؕ يُسَبِّحُ لَهٗ مَا فِى السَّمٰوٰتِ وَالْاَرْضِ ۚ وَهُوَ الْعَزِيْزُ الْحَكِيْمُ ﴿٢٤﴾ ع ٣ ٦

25. Yeye ndiye Allah, Mwumbaji, Mtengenezaji, Mfanyaji wa sura; Mwenye majina mazuri; kinamtukuza kilichomo mbinguni na ardhini; naye ni Mwenye ushindi kamili, Mwenye hekima.

Aliyoyatanguliza. Mtu anatakiwa afikiri, tendo hili analotaka kutenda sasa litaleta matokeo gani baadaye. Kama linaelekea kuleta matokeo mabaya aliache. Tena mtu anatakiwa awe na mipango juu ya mambo ya lazima anayotakiwa kuyafanya baadaye ili wakati wake upite juu ya mambo hasa yenye maana.

Aya 24. *Jabbaar,* neno hili ni sifa ya Allah yenye maana ya Anayeongoa vinavyoharibika.

سُوْرَةُ الْمُمْتَحِنَةِ مَدَنِيَّةٌ وَّ هِيَ مَعَ الْبَسْمَلَةِ اَرْبَعَ عَشْرَةَ اٰيَةً وَّ رُكُوْعَانِ

60. SURA AL-MUMTAHANA

Imeteremshwa Madina

Ina mafungu 2 na Aya 14 pamoja na Bismillahi

بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ ①

1. Kwa jina la Allah, Mwingi wa rehema, Mwingi wa ukarimu.

يٰٓاَيُّهَا الَّذِيْنَ اٰمَنُوْا لَا تَتَّخِذُوْا عَدُوِّيْ وَعَدُوَّكُمْ اَوْلِيَآءَ تُلْقُوْنَ اِلَيْهِمْ بِالْمَوَدَّةِ وَقَدْ كَفَرُوْا بِمَا جَآءَكُمْ مِّنَ الْحَقِّ ۚ يُخْرِجُوْنَ الرَّسُوْلَ وَاِيَّاكُمْ اَنْ تُؤْمِنُوْا بِاللّٰهِ رَبِّكُمْ ؕ اِنْ كُنْتُمْ خَرَجْتُمْ جِهَادًا فِيْ سَبِيْلِيْ وَابْتِغَآءَ مَرْضَاتِيْ ۚ تُسِرُّوْنَ اِلَيْهِمْ بِالْمَوَدَّةِ ۚ وَاَنَا اَعْلَمُ بِمَآ اَخْفَيْتُمْ وَمَآ اَعْلَنْتُمْ ؕ وَمَنْ يَّفْعَلْهُ مِنْكُمْ فَقَدْ ضَلَّ سَوَآءَ السَّبِيْلِ ②

2. Enyi mlioamini, msiwashike adui Zangu na adui zenu kuwa marafiki; mnawapelekea ujumbe wa upendo hali wamekwisha kataa haki iliyowafikieni, wanamfukuza Mtume na ninyi kwa sababu mnamwamini Allah, Mola wenu. Kama mnaondoka kufanya jihadi katika njia Yangu na kuitafuta radhi Yangu, pamoja na hayo mnawatumia kwa siri ujumbe wa upendo, ilhali Mimi Najua zaidi kuliko wote yale mnayoyaficha na mnayoyadhihirisha; (Hivyo harakati zenu hizi za siri hazina faida) na anayefanya hayo miongoni mwenu, basi amekwisha kupotea njia iliyo sawa.

اِنْ يَّثْقَفُوْكُمْ يَكُوْنُوْا لَكُمْ اَعْدَآءً وَّيَبْسُطُوْٓا اِلَيْكُمْ اَيْدِيَهُمْ وَاَلْسِنَتَهُمْ بِالسُّوْٓءِ وَوَدُّوْا لَوْ تَكْفُرُوْنَ ③

3. Wakiwakuteni popote pale wataendelea tu kuwa maadui zenu, na watawakunjulieni mikono yao na ndimi zao kwa uovu, na watapenda laiti na nyinyi pia mkatae.

لَنْ تَنْفَعَكُمْ اَرْحَامُكُمْ وَلَآ اَوْلَادُكُمْ ۚ يَوْمَ الْقِيٰمَةِ ۚ يَفْصِلُ بَيْنَكُمْ ؕ وَاللّٰهُ بِمَا تَعْمَلُوْنَ بَصِيْرٌ ④

4. Hawatawafalieni ndugu zenu wala watoto wenu siku ya Kiyama; Atahukumu baina yenu, na Allah Huyaona mnayoyatenda.

Sura hii nzima inaeleza uhusiano ulio baina ya Waislamu na wasio Waislamu, na inaeleza jinsi lisivyo jambo zuri kufanya urafiki na maadui wanaotaka kuangamiza Uislamu na kuwafanyia vita Waislamu. Mtume *s.a.w.* alikuwa akiwajaribu wanawake waliofika Madina kutoka Makka waliotaka kuingia Uislamu ili kujua kama ni kweli wana nia safi na walipoonekana wana nia safi hawakurudishwa Makka kwa makafiri. Sura hii ilishuka Madina yumkini katika mwaka wa 8.

Aya 2. Waislamu wamekatazwa kufanya urafiki na maadui wa Uislamu wakati maadui hao wanapokuwa katika hali ya vita na Waislamu, na Aya 9 na 10 inahakikisha jambo hili.

قَدْ كَانَتْ لَكُمْ اُسْوَةٌ حَسَنَةٌ فِيْٓ اِبْرٰهِيْمَ
وَالَّذِيْنَ مَعَهٗ ۚ اِذْ قَالُوْا لِقَوْمِهِمْ اِنَّا
بُرَءٰٓؤُا مِنْكُمْ وَمِمَّا تَعْبُدُوْنَ مِنْ دُوْنِ
اللّٰهِ ۫ كَفَرْنَا بِكُمْ وَبَدَا بَيْنَنَا وَبَيْنَكُمُ
الْعَدَاوَةُ وَالْبَغْضَآءُ اَبَدًا حَتّٰى تُؤْمِنُوْا
بِاللّٰهِ وَحْدَهٗٓ اِلَّا قَوْلَ اِبْرٰهِيْمَ لِاَبِيْهِ
لَاَسْتَغْفِرَنَّ لَكَ وَمَآ اَمْلِكُ لَكَ
مِنَ اللّٰهِ مِنْ شَيْءٍ ؕ رَبَّنَا عَلَيْكَ تَوَكَّلْنَا
وَاِلَيْكَ اَنَبْنَا وَاِلَيْكَ الْمَصِيْرُ ۝

5. Hakika ulikuwa mfano mzuri kwenu kwa Ibrahimu na wale waliokuwa pamoja naye, walipowaambia watu wao: Kwa yakini sisi tu mbali nanyi na hayo mnayoyaabudu kinyume cha Allah; twawakataeni, na umetokea uadui na bughudha ya kudumu kati yenu na yetu mpaka mumwamini Allah peke Yake - ila usemi wa Ibrahimu kwa baba yake: Hakika nitakuombea msamaha, wala sina hiari yoyote kwa ajili yako mbele ya Allah. Mola wetu! tumetegemea Kwako, na tumegeukia Kwako, na Kwako ni marejeo.

رَبَّنَا لَا تَجْعَلْنَا فِتْنَةً لِّلَّذِيْنَ كَفَرُوْا
وَاغْفِرْ لَنَا رَبَّنَا ۚ اِنَّكَ اَنْتَ الْعَزِيْزُ
الْحَكِيْمُ ۝

6. Mola wetu, Usitufanye jaribio kwa wale waliokufuru, na Utughofiri, Mola wetu, hakika Wewe ni Mwenye nguvu, Mwenye hekima.

لَقَدْ كَانَ لَكُمْ فِيْهِمْ اُسْوَةٌ حَسَنَةٌ لِّمَنْ
كَانَ يَرْجُوا اللّٰهَ وَالْيَوْمَ الْاٰخِرَ ؕ وَمَنْ
يَّتَوَلَّ فَاِنَّ اللّٰهَ هُوَ الْغَنِيُّ الْحَمِيْدُ ۝ ع

7. Kwa yakini ulikuwa mfano mwema kwenu katika mwenendo wao, kwa anayemtarajia Allah na siku ya Mwisho; na anayekengeuka, basi kwa hakika Allah ni Mkwasi, Asifiwaye.

FUNGU 2

عَسَى اللّٰهُ اَنْ يَّجْعَلَ بَيْنَكُمْ وَبَيْنَ الَّذِيْنَ
عَادَيْتُمْ مِّنْهُمْ مَّوَدَّةً ؕ وَاللّٰهُ قَدِيْرٌ ؕ
وَاللّٰهُ غَفُوْرٌ رَّحِيْمٌ ۝

8. Asaa Allah Akaweka mapenzi baina yenu na wale ambao mnawaona kuwa maadui miongoni mwao; na Allah ni Mwenye kudra; na Allah ni Msamehevu, Mrehemevu.

لَا يَنْهٰىكُمُ اللّٰهُ عَنِ الَّذِيْنَ لَمْ
يُقَاتِلُوْكُمْ فِى الدِّيْنِ وَلَمْ يُخْرِجُوْكُمْ
مِّنْ دِيَارِكُمْ اَنْ تَبَرُّوْهُمْ وَتُقْسِطُوْٓا

9. Allah Hawakatazeni wale ambao hawakupigana nanyi kwa ajili ya dini wala hawakuwafukuzeni katika nyumba zenu ya kwamba

mwafanyie hisani na uadilifu. Hakika Allah Huwapenda wafanyao uadilifu.

10. Allah Anawakatazeni kufanya urafiki na wale tu ambao walipigana nanyi katika dini, na kuwafukuzeni katika nyumba zenu, na wakasaidiana katika kuwafukuzeni. Na wafanyao urafiki nao basi hao ndio wadhalimu.

11. Enyi mlioamini, watakapowafikieni wanawake waaminio wanaohama, basi wajaribuni, Allah ndiye Ajuaye zaidi imani yao, kama mkijua kuwa wao ni waaminio basi msiwarudishe kwa makafiri. (Wanawake) hawa si halali kwao, wala wao (wanaume makafiri) si halali kwao; na warudishieni (mawalii wao) mali walizotoa. Wala kwenu si dhambi kuwaoa maadam mmeshawapa mahari yao; wala msijichukulie mamlaka ya kusimamia ndoa za wanawake makafiri, na ombeni vile mlivyowagharamia, nao wawaombeni walivyogharamia. Hii ndiyo hukumu ya Allah Anayohukumu kati yenu; na Allah ndiye Ajuaye, Mwenye hekima.

12. Na kama akiondoka ye yote katika wake zenu kwenda kwa makafiri, na mmeisha chukua fidia , basi wapeni wale ambao wake zao wamekwisha kwenda, sawa na walichokitoa, na Mcheni Allah Ambaye mnamwamini.

اِلَيْهِمْ ؕ اِنَّ اللّٰهَ يُحِبُّ الْمُقْسِطِيْنَ ۝٩

اِنَّمَا يَنْهٰىكُمُ اللّٰهُ عَنِ الَّذِيْنَ قٰتَلُوْكُمْ فِى الدِّيْنِ وَ اَخْرَجُوْكُمْ مِّنْ دِيَارِكُمْ وَظٰهَرُوْا عَلٰٓى اِخْرَاجِكُمْ اَنْ تَوَلَّوْهُمْ ۚ وَ مَنْ يَّتَوَلَّهُمْ فَاُولٰٓئِكَ هُمُ الظّٰلِمُوْنَ ۝١٠

يٰٓاَيُّهَا الَّذِيْنَ اٰمَنُوْٓا اِذَا جَآءَكُمُ الْمُؤْمِنٰتُ مُهٰجِرٰتٍ فَامْتَحِنُوْهُنَّ ؕ اَللّٰهُ اَعْلَمُ بِاِيْمَانِهِنَّ ۚ فَاِنْ عَلِمْتُمُوْهُنَّ مُؤْمِنٰتٍ فَلَا تَرْجِعُوْهُنَّ اِلَى الْكُفَّارِ ؕ لَا هُنَّ حِلٌّ لَّهُمْ وَلَا هُمْ يَحِلُّوْنَ لَهُنَّ ؕ وَاٰتُوْهُمْ مَّآ اَنْفَقُوْا ؕ وَلَا جُنَاحَ عَلَيْكُمْ اَنْ تَنْكِحُوْهُنَّ اِذَآ اٰتَيْتُمُوْهُنَّ اُجُوْرَهُنَّ ؕ وَلَا تُمْسِكُوْا بِعِصَمِ الْكَوَافِرِ وَسْـَٔلُوْا مَآ اَنْفَقْتُمْ وَلْيَسْـَٔلُوْا مَآ اَنْفَقُوْا ؕ ذٰلِكُمْ حُكْمُ اللّٰهِ ؕ يَحْكُمُ بَيْنَكُمْ ؕ وَاللّٰهُ عَلِيْمٌ حَكِيْمٌ ۝١١

وَاِنْ فَاتَكُمْ شَىْءٌ مِّنْ اَزْوَاجِكُمْ اِلَى الْكُفَّارِ فَعَاقَبْتُمْ فَاٰتُوا الَّذِيْنَ ذَهَبَتْ اَزْوَاجُهُمْ مِّثْلَ مَآ اَنْفَقُوْا ؕ وَاتَّقُوا اللّٰهَ الَّذِىْٓ اَنْتُمْ بِهٖ مُؤْمِنُوْنَ ۝١٢

13. Ewe Nabii! Wakujiapo wanawake walioamini na kufanya baiat yako katika jambo hili kwamba hawatamshirikisha Allah na cho chote, wala hawataiba, wala hawatazini, wala hawatawauwa watoto wao, wala hawataleta uzushi waliouzusha wenyewe, wala hawatakuasi katika mambo mema, basi chukua baiat yao na uwatakie ghofira kwa Allah. Hakika Allah ni Mwingi wa ghofira, Mwingi wa rehema.

يٰٓاَيُّهَا النَّبِيُّ اِذَا جَآءَكَ الْمُؤْمِنٰتُ
يُبَايِعْنَكَ عَلٰٓى اَنْ لَّا يُشْرِكْنَ بِاللّٰهِ شَيْـًٔا
وَّلَا يَسْرِقْنَ وَلَا يَزْنِيْنَ وَلَا يَقْتُلْنَ
اَوْلَادَهُنَّ وَلَا يَاْتِيْنَ بِبُهْتَانٍ يَّفْتَرِيْنَهٗ
بَيْنَ اَيْدِيْهِنَّ وَاَرْجُلِهِنَّ وَلَا يَعْصِيْنَكَ
فِيْ مَعْرُوْفٍ فَبَايِعْهُنَّ وَاسْتَغْفِرْ لَهُنَّ
اللّٰهَ ؕ اِنَّ اللّٰهَ غَفُوْرٌ رَّحِيْمٌ ﴿١٣﴾

14. Enyi mlioamini! Msifanye urafiki na watu ambao Allah Amewakasirikia; maana wamekata tamaa ya Akhera kama vile makafiri walivyowakatia tamaa watu wa makaburini.

يٰٓاَيُّهَا الَّذِيْنَ اٰمَنُوْا لَا تَتَوَلَّوْا قَوْمًا
غَضِبَ اللّٰهُ عَلَيْهِمْ قَدْ يَئِسُوْا مِنَ
الْاٰخِرَةِ كَمَا يَئِسَ الْكُفَّارُ مِنْ
اَصْحٰبِ الْقُبُوْرِ ﴿١٤﴾ ع ٢ ٧ ٨ النصف

Aya 13. *Hawatakuasi katika jambo jema,* sio mradi wake ya kuwa nabii anaweza kutoa jambo baya, la, bali inaonyesha ya kuwa jambo linalotolewa na Nabii huwa jema na huleta manufaa kama litafuatwa inavyotakiwa.

سُوْرَةُ الصَّفِّ مَدَنِيَّةٌ وَّ هِيَ مَعَ الْبَسْمَلَةِ خَمْسَ عَشْرَةَ اٰيَةً وَّ رُكُوْعَانِ

61. SURA AS-SAF

Imeteremshwa Madina

Ina mafungu 2 na Aya 15 pamoja na Bismillahi

بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ ①

1. Kwa jina la Allahu, Mwingi wa rehema, Mwingi wa ukarimu.

سَبَّحَ لِلّٰهِ مَا فِي السَّمٰوٰتِ وَمَا فِي الْاَرْضِ ۚ وَهُوَ الْعَزِيْزُ الْحَكِيْمُ ②

2. Vinamtukuza Allah vilivyomo mbinguni na vilivyomo ardhini; na yeye ni Mwenye ushindi kamili, Mwenye hekima.

يٰٓاَيُّهَا الَّذِيْنَ اٰمَنُوْا لِمَ تَقُوْلُوْنَ مَا لَا تَفْعَلُوْنَ ③

3. Enyi mlioamini! mbona mnasema msiyoyatenda?

كَبُرَ مَقْتًا عِنْدَ اللّٰهِ اَنْ تَقُوْلُوْا مَا لَا تَفْعَلُوْنَ ④

4. Ni dhambi kubwa mbele ya Allah kusema msiyoyatenda.

اِنَّ اللّٰهَ يُحِبُّ الَّذِيْنَ يُقَاتِلُوْنَ فِيْ سَبِيْلِهٖ صَفًّا كَاَنَّهُمْ بُنْيَانٌ مَّرْصُوْصٌ ⑤

5. Kwa yakini Allah Huwapenda wale wanaopigana katika njia Yake safusafu kana kwamba wao ni jengo lililojengwa kwa risasi.

وَاِذْ قَالَ مُوْسٰى لِقَوْمِهٖ يٰقَوْمِ لِمَ تُؤْذُوْنَنِيْ وَقَدْ تَّعْلَمُوْنَ اَنِّيْ رَسُوْلُ اللّٰهِ اِلَيْكُمْ ؕ فَلَمَّا زَاغُوْٓا اَزَاغَ اللّٰهُ قُلُوْبَهُمْ ؕ وَاللّٰهُ لَا يَهْدِي الْقَوْمَ الْفٰسِقِيْنَ ⑥

6. Na Musa alipowaambia watu wake: Enyi watu wangu, mbona mnaniudhi hali mnajua kuwa mimi ni Mtume wa Allah kwenu? Lakini walipopindama, Allah Akaipinda mioyo yao, na Allah Hawaongozi watu wavunjao amri.

Sura hii imeitwa *Safu* kwa sababu ya maagizo wanayopewa Waislamu ndani ya sura hii wasimame safu wanapokuwa wakipigana na adui kwa kuilinda dini yao. Sura hii ilishuka Madina labda katika mwaka wa 4 baada ya Hijra, nayo ilishuka baada ya Waislamu kushindwa katika vita vya Uhud.

Aya 3. Habari hizi hasa wanaambiwa Waislamu wa siku za mwisho ya kuwa wasiseme wasiyoyatenda, na wasiseme vingine na kutenda vingine. Mwendo wa namna hii ni mbaya sana na wanaonywa wasiushike.

7. Na aliposema Isa bin Mariamu: Enyi wana wa Israeli, mimi ni Mtume wa Allah kwenu, nisadikishaye yaliyo mbele yangu katika Taurati na kutoa habari njema ya Mtume atakayefika nyuma yangu jina lake ni Ahmad; lakini alipowafikia kwa Ishara zilizo wazi, wakasema: Huu ni udanganyifu dhahiri.

وَاِذْ قَالَ عِيْسَى ابْنُ مَرْيَمَ يٰبَنِيْٓ اِسْرَآءِيْلَ اِنِّيْ رَسُوْلُ اللّٰهِ اِلَيْكُمْ مُّصَدِّقًا لِّمَا بَيْنَ يَدَيَّ مِنَ التَّوْرٰىةِ وَمُبَشِّرًا بِرَسُوْلٍ يَّاْتِيْ مِنْۢ بَعْدِي اسْمُهٗٓ اَحْمَدُ ؕ فَلَمَّا جَآءَهُمْ بِالْبَيِّنٰتِ قَالُوْا هٰذَا سِحْرٌ مُّبِيْنٌ ۝٧

8. Na ni nani mdhalimu mkubwa kuliko yule anayemzulia Allah uwongo na hali anaitwa kwenye Uislamu? Na Allah Hawaongozi watu wadhalimu.

وَمَنْ اَظْلَمُ مِمَّنِ افْتَرٰى عَلَى اللّٰهِ الْكَذِبَ وَهُوَ يُدْعٰٓى اِلَى الْاِسْلَامِ ؕ وَاللّٰهُ لَا يَهْدِي الْقَوْمَ الظّٰلِمِيْنَ ۝٨

9. Wanataka kuizima nuru ya Allah kwa kuipuliza kwa vinywa vyao, ilhali Allah ni Mwenye kuikamilisha nuru Yake katika kila hali, ijapokuwa makafiri wakirihike.

يُرِيْدُوْنَ لِيُطْفِـُٔوْا نُوْرَ اللّٰهِ بِاَفْوَاهِهِمْ وَاللّٰهُ مُتِمُّ نُوْرِهٖ وَلَوْ كَرِهَ الْكٰفِرُوْنَ ۝٩

10. Yeye ndiye Aliyemtuma Mtume Wake kwa mwongozo na kwa dini ya haki ili kuifanya izishinde dini zote ijapokuwa washirikina wachukie.

هُوَ الَّذِيْٓ اَرْسَلَ رَسُوْلَهٗ بِالْهُدٰى وَدِيْنِ الْحَقِّ لِيُظْهِرَهٗ عَلَى الدِّيْنِ كُلِّهٖ ۙ وَلَوْ كَرِهَ الْمُشْرِكُوْنَ ۝١٠ ع ١

FUNGU 2

11. Enyi mlioamini! je, Niwajulisheni biashara itakayowaokoeni katika adhabu iumizayo?

يٰٓاَيُّهَا الَّذِيْنَ اٰمَنُوْا هَلْ اَدُلُّكُمْ عَلٰى تِجَارَةٍ تُنْجِيْكُمْ مِّنْ عَذَابٍ اَلِيْمٍ ۝١١

12. Mwaminini Allah na Mtume Wake, na jitahidini katika njia ya Allah kwa mali zenu na nafsi zenu; hayo ni bora kwenu ikiwa mnajua.

تُؤْمِنُوْنَ بِاللّٰهِ وَرَسُوْلِهٖ وَتُجَاهِدُوْنَ فِيْ سَبِيْلِ اللّٰهِ بِاَمْوَالِكُمْ وَاَنْفُسِكُمْ ؕ ذٰلِكُمْ خَيْرٌ لَّكُمْ اِنْ كُنْتُمْ تَعْلَمُوْنَ ۝١٢

Aya 10. Karibu mufasirina wote wanakubaliana ya kuwa ushindi uliobashiriwa katika Aya hii utatimia katika wakati wa Masihi Aliyeahidiwa (Ibn Jarir jalada 10; Razi). Na katika Hadithi imesimuliwa ya kuwa katika wakati wa Masihi Aliyeahidiwa zitaangamizwa dini zote isipokuwa Uislamu (Abu Dawud jalada 2).

يَغْفِرْ لَكُمْ ذُنُوْبَكُمْ وَيُدْخِلْكُمْ جَنّٰتٍ
تَجْرِيْ مِنْ تَحْتِهَا الْاَنْهٰرُ وَمَسٰكِنَ
طَيِّبَةً فِيْ جَنّٰتِ عَدْنٍ ؕ ذٰلِكَ الْفَوْزُ
الْعَظِيْمُ ۙ﴿۱۲﴾

13. Atawasameheni dhambi zenu na Atawaingizeni katika Bustani zipitazo mito ndani yake, na makao mazuri katika Bustani za milele: haya ni mafanikio makubwa sana.

وَاُخْرٰى تُحِبُّوْنَهَا ؕ نَصْرٌ مِّنَ اللّٰهِ وَفَتْحٌ
قَرِيْبٌ ؕ وَبَشِّرِ الْمُؤْمِنِيْنَ﴿۱۳﴾

14. Na kingine mnachokipenda: msaada utokao kwa Allah na ushindi ulio karibu! Na uwapashe habari njema waaminio.

يٰۤاَيُّهَا الَّذِيْنَ اٰمَنُوْا كُوْنُوْۤا اَنْصَارَ اللّٰهِ كَمَا
قَالَ عِيْسَى ابْنُ مَرْيَمَ لِلْحَوَارِيّٖنَ مَنْ
اَنْصَارِيْۤ اِلَى اللّٰهِ ؕ قَالَ الْحَوَارِيُّوْنَ
نَحْنُ اَنْصَارُ اللّٰهِ فَاٰمَنَتْ طَّآئِفَةٌ مِّنْۢ
بَنِيْۤ اِسْرَآءِيْلَ وَ كَفَرَتْ طَّآئِفَةٌ ۚ
فَاَيَّدْنَا الَّذِيْنَ اٰمَنُوْا عَلٰى عَدُوِّهِمْ
فَاَصْبَحُوْا ظٰهِرِيْنَ﴿۱۴﴾ ع ۲

15. Enyi mlioamini! Kuweni wasaidizi wa Allah, kama alivyosema Isa bin Mariamu kuwaambia wanafunzi (wake): Ni nani wasaidizi wangu kwa ajili ya Allah? Wanafunzi wakasema: Sisi ni wasaidizi wa Allah. Basi taifa moja la wana wa Israeli waliamini na taifa jingine wakakufuru; ndipo Tukawasaidia wale walioamini dhidi ya maadui zao, na wakawa wenye kushinda.

سُوْرَةُ الْجُمُعَةِ مَدَنِيَّةٌ وَّ هِيَ مَعَ الْبَسْمَلَةِ اثْنَتَا عَشْرَةَ اٰيَةً وَّ رُكُوْعَانِ

62. SURA AL-JUMU'A

Imetereshwa Madina

Ina mafungu 2 na Aya 12 pamoja na Bismillahi

بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ ①

1. Kwa jina la Allah, Mwingi wa rehema, Mwingi wa ukarimu.

يُسَبِّحُ لِلّٰهِ مَا فِي السَّمٰوٰتِ وَمَا فِي الْاَرْضِ الْمَلِكِ الْقُدُّوْسِ الْعَزِيْزِ الْحَكِيْمِ ②

2. Vilivyomo katika mbingu na vilivyomo katika ardhi vinamtukuza Allah, Mfalme, Mtakatifu, Mwenye ushindi kamili, Mwenye hekima.

هُوَ الَّذِيْ بَعَثَ فِي الْاُمِّيّٖنَ رَسُوْلًا مِّنْهُمْ يَتْلُوْا عَلَيْهِمْ اٰيٰتِهٖ وَيُزَكِّيْهِمْ وَيُعَلِّمُهُمُ الْكِتٰبَ وَالْحِكْمَةَ ۗ وَاِنْ كَانُوْا مِنْ قَبْلُ لَفِيْ ضَلٰلٍ مُّبِيْنٍ ۙ ③

3. Yeye ndiye Aliyemwinua Mtume katika watu wasiojua kusoma, atokaye miongoni mwao, anawasomea Aya Zake na kuwatakasa na kuwafunza Kitabu na Hekima, na ingawa hapo kabla kwa hakika walikuwa katika upotevu dhahiri.

وَّاٰخَرِيْنَ مِنْهُمْ لَمَّا يَلْحَقُوْا بِهِمْ ؕ وَهُوَ الْعَزِيْزُ الْحَكِيْمُ ④

4. Na kwa wengine miongoni mwao walio bado kuungana nao; na Yeye ni Mwenye ushindi kamili, Mwenye hekima.

ذٰلِكَ فَضْلُ اللّٰهِ يُؤْتِيْهِ مَنْ يَّشَآءُ ؕ وَاللّٰهُ ذُو الْفَضْلِ الْعَظِيْمِ ⑤

5. Hiyo ni fadhili ya Allah Atampa Amtakaye; na Allah ni Mwenye fadhili kuu.

Sura hii imepata jina katika maagizo ya kukusanyika kwa ajili ya Sala ya Ijumaa. Sura hii ilishuka Madina, yumkini katika mwaka wa pili wa Hijra.

Aya 4. *Na wengine miongoni mwao walio bado kuungana nao.* Abu Huraira anasimulia na nasema: "Tulikuwa tunakaa pamoja na Mtume *s.a.w.* iliposhushwa sura *Jumu'ah* kwa Mtume, na maneno haya yalikuwamo ndani yake: *Na kwa wengine miongoni mwao walio bado kuungana nao.* Nikamwuliza Mtume, 'Ni nani hao?' Hakujibu mpaka nilipomwuliza mara tatu. salman, Mwajemi, alikuwa pamoja nasi, na Mtume *s.a.w.* aliweka mkono wake juu ya Salma akasema; "Hata kama imani ingetungikwa kwenye kilimia, watu au mtu katika hawa ataipata'" (Bukhari).

Bishara iliyomo katika Aya na Hadithi hii imekwisha timia. Seyidna Ahmad ambaye jadi yake ni Mwajemi ametangaza kwa amri ya Allah kuwa amepewa cheo cha Masihi na Mahdi ili kuuimarisha Uislamu , na wafuasi wake ndio hao waliotajwa katika Aya hiyo ambao walisemwa watakuwa miongoni mwa masahaba wa Mtume *s.a.w.* kwa kumkubali Mjumbe aliyeahidiwa.

مَثَلُ الَّذِيْنَ حُمِّلُوا التَّوْرٰىةَ ثُمَّ
لَمْ يَحْمِلُوْهَا كَمَثَلِ الْحِمَارِ يَحْمِلُ
اَسْفَارًا ؕ بِئْسَ مَثَلُ الْقَوْمِ الَّذِيْنَ
كَذَّبُوْا بِاٰيٰتِ اللّٰهِ ؕ وَاللّٰهُ لَا يَهْدِى
الْقَوْمَ الظّٰلِمِيْنَ ۝٦

6. Mfano wa wale waliopewa Taurati kisha hawakuitekeleza (kama inavyostahili) ni kama mfano wa punda anayebeba vitabu vikubwa vikubwa; ni mbaya kiasi gani mfano wa watu wale waliozikadhibisha Aya za Allah; Na Allah Hawaongozi watu wadhalimu.

قُلْ يٰٓاَيُّهَا الَّذِيْنَ هَادُوْٓا اِنْ زَعَمْتُمْ
اَنَّكُمْ اَوْلِيَآءُ لِلّٰهِ مِنْ دُوْنِ النَّاسِ
فَتَمَنَّوُا الْمَوْتَ اِنْ كُنْتُمْ صٰدِقِيْنَ ۝٧

7. Sema: Enyi Mayahudi, kama mnadhani ya kuwa ni ninyi tu ndio wapenzi wa Allah minghairi ya watu wengine wote, basi itamanini mauti ikiwa ninyi ni wakweli.

وَلَا يَتَمَنَّوْنَهٗٓ اَبَدًۢا بِمَا قَدَّمَتْ اَيْدِيْهِمْ ؕ
وَاللّٰهُ عَلِيْمٌۢ بِالظّٰلِمِيْنَ ۝٨

8. Lakini hawataitamani kamwe kwa sababu ya yale iliyoyatanguliza mikono yao; na Allah Anawajua wadhalimu.

قُلْ اِنَّ الْمَوْتَ الَّذِىْ تَفِرُّوْنَ مِنْهُ فَاِنَّهٗ
مُلٰقِيْكُمْ ثُمَّ تُرَدُّوْنَ اِلٰى عٰلِمِ الْغَيْبِ
وَالشَّهَادَةِ فَيُنَبِّئُكُمْ بِمَا كُنْتُمْ تَعْمَلُوْنَ ۝٩ ع

9. Sema: Hakika mauti yale mnayoyakimbia, bila shaka yatawakamateni, kisha mtarudishwa kwa Mjuzi wa siri na dhahiri, ndipo Atawaambieni mliyokuwa mkiyatenda.

FUNGU 2

يٰٓاَيُّهَا الَّذِيْنَ اٰمَنُوْٓا اِذَا نُوْدِىَ لِلصَّلٰوةِ
مِنْ يَّوْمِ الْجُمُعَةِ فَاسْعَوْا اِلٰى ذِكْرِ اللّٰهِ
وَذَرُوا الْبَيْعَ ؕ ذٰلِكُمْ خَيْرٌ لَّكُمْ اِنْ كُنْتُمْ
تَعْلَمُوْنَ ۝١٠

10. Enyi mlioamini! Inaponadiwa kwa ajili ya Sala katika wakati fulani wa siku ya Ijumaa, basi nendeni haraka kumkumbuka Allah na acheni biashara; hiyo ni bora kwenu ikiwa mnajua.

Aya 10. Nendeni upesi. Amri hii inaonyesha ya kuwa Sala ya Ijumaa imetiliwa mkazo sana; na kwa hakika toka mwanzo Waislamu waliifahamu siku hii kama Idi yao. Mtume s.a.w. alisema, "Afadhali watu wajiepushe na kutohudhuria Sala ya Ijumaa, isije Allah akapiga muhuri juu ya nyoyo zao, kisha wakawa miongoni mwa walioghafilika" (Muslim).

Sala ya kwanza ya Ijumaa Mtume alisali Madina katika mtaa wa Banu Salim bin Auf, akatoa hotuba na akasali rakaa mbili; na toka siku hiyo kawaida hii ikaendelea (Ibn Hisham). Mahali pale aliposalia Sala ya Ijumaa baadaye palijengwa msikiti na kwa sababu ya Sala ile ukaitwa Masjid al-Jum'a.

فَاِذَا قُضِيَتِ الصَّلٰوةُ فَانْتَشِرُوْا فِى
الْاَرْضِ وَابْتَغُوْا مِنْ فَضْلِ اللّٰهِ
وَاذْكُرُوا اللّٰهَ كَثِيْرًا لَّعَلَّكُمْ
تُفْلِحُوْنَ ﴿١١﴾

11. Na itakapokwisha Sala, basi tawanyikeni katika ardhi na zitafuteni fadhili za Allah, na Mkumbukeni Allah kwa wingi, ili mpate kufaulu.

وَاِذَا رَاَوْا تِجَارَةً اَوْ لَهْوَا ِۨانْفَضُّوْٓا اِلَيْهَا
وَتَرَكُوْكَ قَآئِمًا ؕ قُلْ مَا عِنْدَ اللّٰهِ خَيْرٌ
مِّنَ اللَّهْوِ وَمِنَ التِّجَارَةِ ؕ وَاللّٰهُ خَيْرُ
الرّٰزِقِيْنَ ﴿١٢﴾ ع ٢/١٢

12. Na watakapoiona biashara au jambo lenye kuwavutia watavikimbilia na watakuacha ukisimama. Sema: Yaliyoko kwa Allah ni bora kuliko mambo yavutiayo na biashara; na Allah ni Mbora wa watoao riziki.

Sala ya Ijumaa husaliwa na Waaminio wasiopungua watatu, mahali po pote watakapokuwa. Siyo lazima waweko watu arubaini wa mjini na sultani. Maneno haya, Ya ayyuhalladhina aamanuu (Enyi mlioamini); yako katika siigha ya uwingi. Na uwingi katika lugha ya Kiarabu huanzia toka idadi ya tatu. Hivyo maneno haya yanaonyesha hakika ya jambo hili. Hakuna haja ya kusali Ijumaa pamoja na Adhuhuri kama wafanyavyo watu wengine. Ijumaa peke yake inatosha.

سُوْرَةُ الْمُنَافِقُوْنَ مَدَنِيَّةٌ وَّ هِيَ مَعَ الْبَسْمَلَةِ اثْنَتَا عَشْرَةَ اٰيَةً وَّ رُكُوْعَانِ

63. SURA AL-MUNAAFIQUUN

Imeteremshwa Madina

Ina mafungu 2 na Aya 12 pamoja na Bismillahi

بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ ①

1. Kwa jina la Allah, Mwingi wa rehema, Mwingi wa ukarimu.

اِذَا جَآءَكَ الْمُنٰفِقُوْنَ قَالُوْا نَشْهَدُ اِنَّكَ لَرَسُوْلُ اللّٰهِ ۘ وَ اللّٰهُ يَعْلَمُ اِنَّكَ لَرَسُوْلُهٗ ؕ وَاللّٰهُ يَشْهَدُ اِنَّ الْمُنٰفِقِيْنَ لَكٰذِبُوْنَ ②

2. Wanapokujia wanafiki, husema: Tunashuhudia ya kuwa kwa yakini wewe ni Mtume wa Allah na Allah Anajua kwa hakika wewe ni Mtume Wake; Na Allah Anashuhudia ya kuwa kwa hakika wanafiki ni waongo.

اِتَّخَذُوْٓا اَيْمَانَهُمْ جُنَّةً فَصَدُّوْا عَنْ سَبِيْلِ اللّٰهِ ؕ اِنَّهُمْ سَآءَ مَا كَانُوْا يَعْمَلُوْنَ ③

3. Wamevifanya viapo vyao kuwa ngao, basi wao wanaizuilia njia ya Allah; kwa hakika ni mabaya waliyokuwa wakiyafanya.

ذٰلِكَ بِاَنَّهُمْ اٰمَنُوْا ثُمَّ كَفَرُوْا فَطُبِعَ عَلٰى قُلُوْبِهِمْ فَهُمْ لَا يَفْقَهُوْنَ ④

4. Hayo ni kwa sababu waliamini kisha wakakufuru, kwa hiyo muhuri umepigwa juu ya mioyo yao nao hawafahamu.

وَ اِذَا رَاَيْتَهُمْ تُعْجِبُكَ اَجْسَامُهُمْ ؕ وَ اِنْ يَّقُوْلُوْا تَسْمَعْ لِقَوْلِهِمْ ؕ كَاَنَّهُمْ خُشُبٌ مُّسَنَّدَةٌ ؕ يَحْسَبُوْنَ كُلَّ صَيْحَةٍ عَلَيْهِمْ ؕ هُمُ الْعَدُوُّ فَاحْذَرْهُمْ ؕ قٰتَلَهُمُ اللّٰهُ ۚ اَنّٰى يُؤْفَكُوْنَ ⑤

5. Na unapowaona, miili yao inakupendeza, na kama wakisema unausikiliza usemi wao; wao ni kama vijiti vilivyoegemezwa; wanaudhani kila mngurumo wa radi ni wenye kuwaangukia. Hao hao ndio maadui, hivyo jihadhari na (shari yao). Laana ya Allah iwe juu yao. Wanageuziwa wapi?

Sura hii nzima inaeleza habari za wanafiki na kuulaumu unafiki. Sura hii ilishuka Makka yumkini katika mwaka wa tatu wa Hijra.

Aya 2. *Wanafiki ni waongo hasa.* Ingawa kauli waliyosema wanafiki kuwa Mtume ni Mjumbe wa Mungu ni ya kweli, lakini Mungu anasema ya kuwa wanasema uwongo, maana maneno yao ni kinyume na itikadi yao na undani wao.

Aya 5. *Kama boriti zilizotegemezwa*. Maneno haya yanaonyesha ilivyo hali ya wanafiki; kama vile boriti haiwezi kusimama yenyewe mpaka itegemee kitu kingine, kadhalika wanafiki katika dhati yao hawana cho chote bali huwa wakitegemea kwa watu wengine.

وَاِذَا قِيْلَ لَهُمْ تَعَالَوْا يَسْتَغْفِرْ لَكُمْ
رَسُوْلُ اللّٰهِ لَوَّوْا رُءُوْسَهُمْ وَرَاَيْتَهُمْ
يَصُدُّوْنَ وَهُمْ مُّسْتَكْبِرُوْنَ ۝٥

6. Na wanapoambiwa: Njooni, Mtume wa Allah atawaombeeni msamaha, huvigeuza vichwa vyao; na unawaona wanajizuia (kuikubali haki) wakitakabari.

سَوَآءٌ عَلَيْهِمْ اَسْتَغْفَرْتَ لَهُمْ اَمْ لَمْ
تَسْتَغْفِرْ لَهُمْ ؕ لَنْ يَّغْفِرَ اللّٰهُ لَهُمْ ؕ
اِنَّ اللّٰهَ لَا يَهْدِى الْقَوْمَ الْفٰسِقِيْنَ ۝٦

7. Ni sawa kwao ukiwatakia msamaha au usiwatakie msamaha, Allah Hatawasamehe; hakika Allah Hawaongozi watu waasi.

هُمُ الَّذِيْنَ يَقُوْلُوْنَ لَا تُنْفِقُوْا عَلٰى مَنْ
عِنْدَ رَسُوْلِ اللّٰهِ حَتّٰى يَنْفَضُّوْا ؕ وَلِلّٰهِ
خَزَآئِنُ السَّمٰوٰتِ وَالْاَرْضِ وَلٰكِنَّ
الْمُنٰفِقِيْنَ لَا يَفْقَهُوْنَ ۝٧

8. Hao ndio wanaosema: Msitoe mali kwa ajili ya wale walio pamoja na Mtume wa Allah mpaka watawanyike. Ilhali hazina za mbingu na ardhi ni za Allah lakini wanafiki hawaelewi.

يَقُوْلُوْنَ لَئِنْ رَّجَعْنَاۤ اِلَى الْمَدِيْنَةِ
لَيُخْرِجَنَّ الْاَعَزُّ مِنْهَا الْاَذَلَّ ؕ وَلِلّٰهِ
الْعِزَّةُ وَلِرَسُوْلِهٖ وَلِلْمُؤْمِنِيْنَ وَلٰكِنَّ
الْمُنٰفِقِيْنَ لَا يَعْلَمُوْنَ ۝٨ ع ١٣

9. Wanasema: Tukirudi Madina, mwenye heshima kuliko wote atamfukuza aliye dhalili kabisa; na heshima hasa ni kwa Allah na kwa Mtume Wake na kwa waaminio; lakini wanafiki hawajui.

Aya 9. *Mwenye heshima atamfukuza mnyonge.* Maneno haya yalisemwa na Abdullah bin Ubayy bin Salul ambaye kabla ya kufika Mtume *s.a.w.* Madina yeye alikuwa mkubwa wa watu hapo, na alipofika Mtume s.a.w. sasa watu wote wakamwelekea Mtume. Yeye alichukia jambo hili la kukosa ukubwa wake, lakini ili asianguke kabisa akaingia Uislamu kiuwongo-uwongo na akatokea kuwa mkubwa wa wanafiki baadaye.

Waislamu walipokuwa katika vita na Banu Mustalik, Abdullah bin Ubayy bin Salul akasema ya kwamba mwenye heshima, yaani yeye atamfukuza mnyonge, yaani Mtume *s.a.w.* Zaid bin Akram alisikia maneno hayo na akayafikisha kwa Mtume *s.a.w.* Alipoulizwa Abdallah bin Ubbay na Mtume, akaruka kabisa kuwa yeye hakusema. Allah akateremsha Aya hii, na ikajulikana kuwa kweli alisema. Basi Seyidna Umar akaomba aruhusiwe kumwua Abdallah, Mtume akakataza. Mwanawe Abdallah ambaye alikuwa mtu mwaminifu sana, akaomba ruhusa yeye aende akamwue baba yake kwa kosa hili alilofanya. Mtume *s.a.w.* akakataa. Basi yule mtoto wa Abdallah akamkuta baba yake njiani, akamzuia na akamshurutisha kwa nguvu ya kuwa hatompa ruhusa

FUNGU 2

يٰٓاَيُّهَا الَّذِيْنَ اٰمَنُوْا لَا تُلْهِكُمْ اَمْوَالُكُمْ وَلَآ اَوْلَادُكُمْ عَنْ ذِكْرِ اللّٰهِ ۚ وَمَنْ يَّفْعَلْ ذٰلِكَ فَاُولٰٓئِكَ هُمُ الْخٰسِرُوْنَ ۝١٠

10. Enyi mlioamini! yasikusahaulisheni mali yenu wala watoto wenu kumkumbuka Allah; na wafanyao hayo, basi hao ndio wenye hasara.

وَاَنْفِقُوْا مِنْ مَّا رَزَقْنٰكُمْ مِّنْ قَبْلِ اَنْ يَّاْتِيَ اَحَدَكُمُ الْمَوْتُ فَيَقُوْلَ رَبِّ لَوْلَآ اَخَّرْتَنِيْٓ اِلٰٓى اَجَلٍ قَرِيْبٍ ۙ فَاَصَّدَّقَ وَاَكُنْ مِّنَ الصّٰلِحِيْنَ ۝١١

11. Na toeni katika yale Tuliyowapeni, kabla mmoja wenu haijamfikia mauti, kisha aseme: Mola wangu, mbona Hukuniakhirishia muda kidogo, nikatoa sadaka na nikawa miongoni mwa watendao mema?

وَلَنْ يُّؤَخِّرَ اللّٰهُ نَفْسًا اِذَا جَآءَ اَجَلُهَا ۭ وَاللّٰهُ خَبِيْرٌۢ بِمَا تَعْمَلُوْنَ ۝١٢ ع ٢

12. Lakini Allah Hataiakhirisha nafsi yo yote inapofika ajali yake, na Allah Anazo habari za mnayoyatenda.

---

kupita mpaka amesema ya kuwa Mtume ndiye mwenye heshima na yeye ni mnyonge. Abdallah bin Ubbay akalazimika kutamka maneno hayo na akamwacha apite (Bukhari, Tirmidh, Sirat Khatamunnabiyyin jalada la 2).

Aya 10. Sasa hapa wanapewa mawaidha waaminio ya kuwa waangalie sana mali zao na watoto wao vitumike katika njia ya Allah asije vikawatia sahau na unafiki ukaanza kuingia mioyoni mwao.

سُوْرَةُ التَّغَابُنِ مَدَنِيَّةٌ وَّ هِيَ مَعَ الْبَسْمَلَةِ تِسْعَ عَشْرَةَ اٰيَةً وَّ رُكُوْعَانِ

64. SURA AT-TAGHAABUN

Imeteremshwa Madina

Ina mafungu 2 na Aya 19 pamoja na Bismillahi

بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ ①

1. Kwa jina la Allah, Mwingi wa rehema, Mwingi wa ukarimu.

يُسَبِّحُ لِلّٰهِ مَا فِي السَّمٰوٰتِ وَمَا فِي الْاَرْضِ ۚ لَهُ الْمُلْكُ وَلَهُ الْحَمْدُ ۖ وَهُوَ عَلٰى كُلِّ شَيْءٍ قَدِيْرٌ ②

2. Kinamtukuza Allah kila kilichomo mbinguni na kilichomo ardhini; ufalme ni Wake, na sifa njema ni Zake, na Yeye ni Mwenye uwezo juu ya kila kitu.

هُوَ الَّذِيْ خَلَقَكُمْ فَمِنْكُمْ كَافِرٌ وَّمِنْكُمْ مُّؤْمِنٌ ؕ وَاللّٰهُ بِمَا تَعْمَلُوْنَ بَصِيْرٌ ③

3. Yeye Ndiye Aliyewaumbeni, kisha baadhi yenu huwa makafiri na baadhi yenu huwa waaminio. Na Allah Huyaona mnayoyafanya.

خَلَقَ السَّمٰوٰتِ وَالْاَرْضَ بِالْحَقِّ وَصَوَّرَكُمْ فَاَحْسَنَ صُوَرَكُمْ ۚ وَاِلَيْهِ الْمَصِيْرُ ④

4. Ameumba mbingu na ardhi kwa haki, na Akazitengeneza sura zenu na kisha sura zenu Akazifanya vizuri, na marudio ni Kwake.

يَعْلَمُ مَا فِي السَّمٰوٰتِ وَالْاَرْضِ وَيَعْلَمُ مَا تُسِرُّوْنَ وَمَا تُعْلِنُوْنَ ؕ وَاللّٰهُ عَلِيْمٌۢ بِذَاتِ الصُّدُوْرِ ⑤

5. (Allah) Anavijua vilivyomo mbinguni na ardhini, na Anayajua mnayoyaficha na mnayoyadhihirisha; na Allah ni Mjuzi wa yaliyomo vifuani.

Watu wamehitilafiana juu ya sura hii kuwa ya Makka au ya Madina. Wengi zaidi wanakubali kuwa ni ya Madina. Habari zilizomo ndani ya sura yenyewe zinaonyesha ya kuwa ni ya mapema kushuka Madina. Wengine wanafikiri kuwa ya Makka kwa vile ilivyoshuka mara tu baada ya Mtume *s.w.a.* kufika Madina.

Aya 3. Hapa Allah anasema ya kuwa amewaumba watu wapate kumwabudu na kumjua,

6. Je! Haikuwafikieni habari ya wale waliokufuru zamani na wakaonja ubaya wa maamuzi yao na wao wana adhabu iumizayo?

اَلَمْ يَاْتِكُمْ نَبَؤُا الَّذِيْنَ كَفَرُوْا مِنْ قَبْلُ ۫ فَذَاقُوْا وَبَالَ اَمْرِهِمْ وَلَهُمْ عَذَابٌ اَلِيْمٌ ۝٦

7. Hayo ni kwa sababu Mitume wao walikuwa wakiwafikia kwa Ishara waziwazi, lakini wakasema: Je, watu watatuongoza? Kwa hiyo wakakataa na wakageuka upande; na Allah si mhitaji, bali Allah ni Ajitoshaye, Asifiwaye.

ذٰلِكَ بِاَنَّهٗ كَانَتْ تَّاْتِيْهِمْ رُسُلُهُمْ بِالْبَيِّنٰتِ فَقَالُوْٓا اَبَشَرٌ يَّهْدُوْنَنَا ۫ فَكَفَرُوْا وَتَوَلَّوْا وَّاسْتَغْنَى اللّٰهُ ؕ وَاللّٰهُ غَنِيٌّ حَمِيْدٌ ۝٧

8. Waliokufuru wanadai kuwa hawatafufuliwa. Sema: Naam! kwa haki ya Mola wangu ninyi lazima mtafufuliwa; kisha lazima mtajulishwa mliyoyatenda; na hayo ni rahisi kwa Allah.

زَعَمَ الَّذِيْنَ كَفَرُوْٓا اَنْ لَّنْ يُّبْعَثُوْا ؕ قُلْ بَلٰى وَرَبِّيْ لَتُبْعَثُنَّ ثُمَّ لَتُنَبَّؤُنَّ بِمَا عَمِلْتُمْ ؕ وَذٰلِكَ عَلَى اللّٰهِ يَسِيْرٌ ۝٨

9. Basi Mwaminini Allah na Mtume Wake na nuru ambayo Tumeiteremsha; na Allah Anazo habari za mnayoyatenda.

فَاٰمِنُوْا بِاللّٰهِ وَرَسُوْلِهٖ وَالنُّوْرِ الَّذِيْٓ اَنْزَلْنَا ؕ وَاللّٰهُ بِمَا تَعْمَلُوْنَ خَبِيْرٌ ۝٩

10. Siku Atakayowakusanyeni kwa ajili ya siku ya Makusanyiko, hiyo ni siku ya kushindwa au kushinda. Na anayemwamini Allah na kufanya wema (Yeye) Atamfutia maovu yake na Atamwingiza ndani ya bustani zipitazo mito ndani yake, watakaa humo milele. Hayo ni mafanikio makubwa.

يَوْمَ يَجْمَعُكُمْ لِيَوْمِ الْجَمْعِ ذٰلِكَ يَوْمُ التَّغَابُنِ ؕ وَمَنْ يُّؤْمِنْۢ بِاللّٰهِ وَيَعْمَلْ صَالِحًا يُّكَفِّرْ عَنْهُ سَيِّاٰتِهٖ وَيُدْخِلْهُ جَنّٰتٍ تَجْرِيْ مِنْ تَحْتِهَا الْاَنْهٰرُ خٰلِدِيْنَ فِيْهَآ اَبَدًا ؕ ذٰلِكَ الْفَوْزُ الْعَظِيْمُ ۝١٠

11. Na wale waliokufuru na wakakadhibisha Aya Zetu, hao ni watu wa Motoni, watakaa humo; nayo ni marudio mabaya.

وَالَّذِيْنَ كَفَرُوْا وَكَذَّبُوْا بِاٰيٰتِنَآ اُولٰٓئِكَ اَصْحٰبُ النَّارِ خٰلِدِيْنَ فِيْهَا ؕ وَبِئْسَ الْمَصِيْرُ ۝١١ ع

Aya 10. *Yaumu at-Taghaabun,* "Siku ya hasara." Siku hiyo ni ya Kiyama, ambayo ni siku udanganyifu utadhihirika ambao watu waliufanya katika "biashara" ya kununua dunia badala ya Akhera, na watalipwa malipo ya udanganyifu huo ambayo yatakuwa hasara kwa ajili ya wanafiki na makafiri.

FUNGU 2

مَآ اَصَابَ مِنۡ مُّصِيۡبَةٍ اِلَّا بِاِذۡنِ اللّٰهِ ؕ وَمَنۡ يُّؤۡمِنۡۢ بِاللّٰهِ يَهۡدِ قَلۡبَهٗ ؕ وَاللّٰهُ بِكُلِّ شَىۡءٍ عَلِيۡمٌ ﴿۱۲﴾

12. Haufiki msiba wo wote ila kwa idhini ya Allah; na anayemwamini Allah Huuongoza moyo wake: Na Allah ni Mjuzi wa kila kitu.

وَاَطِيۡعُوا اللّٰهَ وَاَطِيۡعُوا الرَّسُوۡلَ ۚ فَاِنۡ تَوَلَّيۡتُمۡ فَاِنَّمَا عَلٰى رَسُوۡلِنَا الۡبَلٰغُ الۡمُبِيۡنُ ﴿۱۳﴾

13. Na Mtiini Allah na mtiini Mtume, lakini mkigeuka, basi juu ya Mtume Wetu ni kufikisha tu waziwazi.

اَللّٰهُ لَاۤ اِلٰهَ اِلَّا هُوَ ؕ وَعَلَى اللّٰهِ فَلۡيَتَوَكَّلِ الۡمُؤۡمِنُوۡنَ ﴿۱۴﴾

14. Allah, hakuna aabudiwaye ila Yeye tu; na waaminio wamtegemee Allah tu.

يٰۤاَيُّهَا الَّذِيۡنَ اٰمَنُوۡۤا اِنَّ مِنۡ اَزۡوَاجِكُمۡ وَاَوۡلَادِكُمۡ عَدُوًّا لَّكُمۡ فَاحۡذَرُوۡهُمۡ ۚ وَاِنۡ تَعۡفُوۡا وَتَصۡفَحُوۡا وَتَغۡفِرُوۡا فَاِنَّ اللّٰهَ غَفُوۡرٌ رَّحِيۡمٌ ﴿۱۵﴾

15. Enyi mlioamini! kwa yakini baadhi ya wake zenu na watoto wenu ni maadui zenu; basi jihadharini nao; na kama mkisamehe na kuvumilia na kughofiri, basi hakika Allah ni Msamehevu, Mwingi wa ukarimu.

اِنَّمَاۤ اَمۡوَالُكُمۡ وَاَوۡلَادُكُمۡ فِتۡنَةٌ ؕ وَاللّٰهُ عِنۡدَهٗۤ اَجۡرٌ عَظِيۡمٌ ﴿۱۶﴾

16. Bila shaka mali zenu na watoto wenu ni jaribio na kwa Allah kuna ujira mkubwa.

فَاتَّقُوا اللّٰهَ مَا اسۡتَطَعۡتُمۡ وَاسۡمَعُوۡا وَاَطِيۡعُوۡا وَاَنۡفِقُوۡا خَيۡرًا لِّاَنۡفُسِكُمۡ ؕ وَمَنۡ يُّوۡقَ شُحَّ نَفۡسِهٖ فَاُولٰٓئِكَ هُمُ الۡمُفۡلِحُوۡنَ ﴿۱۷﴾

17. Kwa hiyo Mcheni Allah mwezavyo, na sikilizeni na tiini na toeni, itakuwa heri kwa nafsi zenu; na aepushwaye na ubahili wa nafsi yake, basi hao ndio wenye kufaulu.

اِنۡ تُقۡرِضُوا اللّٰهَ قَرۡضًا حَسَنًا يُّضٰعِفۡهُ لَكُمۡ وَيَغۡفِرۡ لَكُمۡ ؕ وَاللّٰهُ شَكُوۡرٌ حَلِيۡمٌ ۙ﴿۱۸﴾

18. Mkimkatia Allah sehemu nzuri, Atawazidishieni na Atawaghofirieni, na Allah ni mwenye shukrani, Mpole,

عٰلِمُ الۡغَيۡبِ وَالشَّهَادَةِ الۡعَزِيۡزُ الۡحَكِيۡمُ ﴿۱۹﴾ ع

19. Ajuaye siri na dhahiri, Mwenye ushindi kamili, Mwenye hekima.

Aya 15. Mara nyingi mke na watoto wanakuwa sababu ya kumvutia mtu katika maovu, maana, kwa kutaka kuwaridhi mtu anaanza kuruka mipaka iliyowekwa na Sheria. Uadui wa kidini ambao baadhi ya wakati mtu anaweza kuupata kwa mkewe na watoto ni kitu kinachojulikana sana. Hapa waaminio wanafunzwa kushika hadhari nyingi katika mambo ya wake na watoto.

سُوْرَةُ الطَّلَاقِ مَدَنِيَّةٌ وَّ هِيَ مَعَ الْبَسْمَلَةِ ثَلَاثَ عَشْرَةَ اٰيَةً وَّ رُكُوْعَانِ

65. SURA AT-TALAAQ

Imeteremshwa Madina

Ina mafungu 2 na Aya 13 pamoja na Bismillahi

بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ ①

1. Kwa jina la Allah, Mwingi wa rehema, Mwingi wa ukarimu.

يٰٓاَيُّهَا النَّبِيُّ اِذَا طَلَّقْتُمُ النِّسَآءَ فَطَلِّقُوْهُنَّ لِعِدَّتِهِنَّ وَاَحْصُوا الْعِدَّةَ ۚ وَاتَّقُوا اللّٰهَ رَبَّكُمْ ۚ لَا تُخْرِجُوْهُنَّ مِنْۢ بُيُوْتِهِنَّ وَلَا يَخْرُجْنَ اِلَّآ اَنْ يَّاْتِيْنَ بِفَاحِشَةٍ مُّبَيِّنَةٍ ۭ وَتِلْكَ حُدُوْدُ اللّٰهِ ۭ وَمَنْ يَّتَعَدَّ حُدُوْدَ اللّٰهِ فَقَدْ ظَلَمَ نَفْسَهٗ ۭ لَا تَدْرِيْ لَعَلَّ اللّٰهَ يُحْدِثُ بَعْدَ ذٰلِكَ اَمْرًا ②

2. Ewe Nabii! Mtakapowataliki wanawake, wapeni talaka kwa kuzingatia kipindi cha eda kilichowekwa, na fanyeni hesabu ya kipindi hicho cha eda; na mcheni Allah Mola wenu. Msiwatoe katika nyumba zao wala wasitoke wenyewe, mpaka wafanye jambo la ufasiki ulio wazi. Na hiyo ndiyo mipaka ya Allah; na anayeiruka mipaka ya Allah, basi hakika amejidhulumu nafsi yake. Hujui ya kwamba labda Allah Atatokeza jambo jingine baada ya haya.

فَاِذَا بَلَغْنَ اَجَلَهُنَّ فَاَمْسِكُوْهُنَّ بِمَعْرُوْفٍ اَوْ فَارِقُوْهُنَّ بِمَعْرُوْفٍ وَّاَشْهِدُوْا ذَوَيْ عَدْلٍ مِّنْكُمْ وَاَقِيْمُوا الشَّهَادَةَ لِلّٰهِ ۭ ذٰلِكُمْ يُوْعَظُ بِهٖ مَنْ كَانَ يُؤْمِنُ بِاللّٰهِ وَالْيَوْمِ الْاٰخِرِ ۭ وَمَنْ يَّتَّقِ اللّٰهَ يَجْعَلْ لَّهٗ مَخْرَجًا ③ۙ

3. Basi wanapofikia muda wao, ndipo wawekeni kwa wema, au farakaneni nao kwa wema, na mshuhudishe mashahidi wawili waadilifu miongoni mwenu, na simamisheni ushahidi kwa ajili ya Allah. Hivyo ndivyo anaagizwa yule anayemwamini Allah na siku ya Mwisho; na anayemwogopa Allah, (Allah) Humtengenezea njia ya kuokoka,

---

Sura hii inaeleza habari za talaka katika fungu lake la kwanza, na hivyo imeitwa *Talaka.* Ilishuka Madina karibu katika mwaka wa 6 wa Hijra.

Aya 2. Talaka itolewe mwanamke anapotoka katika hedhi kabla ya kumwingilia na papo hapo inaanza eda yake. Inasimuliwa ya kwamba Abdullah bin Umar alimpa talaka mkewe hali yu

وَّيَرْزُقْهُ مِنْ حَيْثُ لَا يَحْتَسِبُ ؕ وَمَنْ يَّتَوَكَّلْ عَلَى اللّٰهِ فَهُوَ حَسْبُهٗ ؕ اِنَّ اللّٰهَ بَالِغُ اَمْرِهٖ ؕ قَدْ جَعَلَ اللّٰهُ لِكُلِّ شَیْءٍ قَدْرًا ۝٤

4. Na Humpa riziki kwa mahali asipopatazamia; na anayemtegemea Allah, basi Yeye Humtoshea; kwa yakini Allah Hutimiza kusudio Lake. Hakika Allah Amekwisha kiwekea kila kitu kipimo.

وَالّٰٓـِٔیْ یَئِسْنَ مِنَ الْمَحِیْضِ مِنْ نِّسَآىِٕكُمْ اِنِ ارْتَبْتُمْ فَعِدَّتُهُنَّ ثَلٰثَةُ اَشْهُرٍ ۙ وَّالّٰٓـِٔیْ لَمْ یَحِضْنَ ؕ وَاُولَاتُ الْاَحْمَالِ اَجَلُهُنَّ اَنْ یَّضَعْنَ حَمْلَهُنَّ ؕ وَمَنْ یَّتَّقِ اللّٰهَ یَجْعَلْ لَّهٗ مِنْ اَمْرِهٖ یُسْرًا ۝٥

5. Na wale waliokoma hedhi yao miongoni mwa wanawake wenu, ikiwa mnayo shaka, basi muda wa eda yao ni miezi mitatu, na (pia ndiyo eda kwa wale) ambao hawajapata hedhi. Na wanawake wenye mimba eda yao ni mpaka watakapojifungua; na anayemwogopa Allah Humfanyia mambo yake kuwa mepesi.

ذٰلِكَ اَمْرُ اللّٰهِ اَنْزَلَهٗۤ اِلَیْكُمْ ؕ وَمَنْ یَّتَّقِ اللّٰهَ یُكَفِّرْ عَنْهُ سَیِّاٰتِهٖ وَیُعْظِمْ لَهٗۤ اَجْرًا ۝٦

6. Hiyo ni amri ya Allah Aliyoiteremsha kwenu, na anayemwogopa Allah Humfutia maovu yake na Humuongezea sana ujira wake.

---

katika hedhi. Seyidna Umar akapeleka habari hii kwa Mtume *s.a.w.* Mtume akakasirika, akasema, Amrejeshe mkewe, hedhi hii iishe, kisha angoje mpaka hedhi nyingine iishe, na itakapokwisha, basi akitaka ampe talaka, maana hii ndiyo talaka iliyoamrishwa na Allah (Bukhari).

Msiwatoe katika nyumba zao wala wasitoke wenyewe. Amri hii inaonyesha ya kuwa mwanamke hana ruhusa kuondoka au kuondolewa nyumbani mwa mume wake mpaka eda imekwisha. Desturi inayofanywa nchi hii, wanawake kufunga mizigo na kutoka majumbani baada ya kupewa talaka au wanaume kuwatoa imelaumiwa.

Kumpa mwanamke talaka kumeruhusiwa na Sheria ya Kiislamu. Torati pia inahalalisha talaka. Injili inataja uzinifu kuwa sababu ya pekee ya talaka (Matt. 5:32). Wakristo wa siku hizi wanaona kuwa ni dhambi kubwa kumwacha mwanamke kwa sababu yo yote. Yawezekana kutokea maneno mengi yenye kuchafua raha na utulivu wa nyumbani. Taabu hii imefanya mataifa ya Kikristo kupuuza amri ya dini yao na mabaraza yao ya sheria huko Ulaya na Amerika yametoa sababu nyingi mno za ruhusa ya kutoa talaka.

Atatokeza jambo jingine, yaani huenda watarejeana. Hapa ikumbukwe ya kuwa kurejeana hakuji kama mwanamke amekwisha pewa talaka ya tatu.

Aya 6. Katika Aya hii na Aya mbili zilizopita, watu wanaoogopa ubaya kwa kumcha Allah wameahidiwa kupewa mambo matatu: (1) kutengenezewa njia ya kuokoka; (2) kufanyiwa mambo yao kuwa mepesi; (3) kufutiwa maovu yao na kupewa ujira mkuu.

Seyidna Ahmad amesema, "Kumcha Mungu ndio msingi wa kila heri, kama msingi huu umesalimika basi kila kitu kimesalimika" (Durri Thamin).

اَسْكِنُوْهُنَّ مِنْ حَيْثُ سَكَنْتُمْ مِّنْ
وُّجْدِكُمْ وَلَا تُضَآرُّوْهُنَّ لِتُضَيِّقُوْا
عَلَيْهِنَّ ؕ وَاِنْ كُنَّ اُولَاتِ حَمْلٍ
فَاَنْفِقُوْا عَلَيْهِنَّ حَتّٰى يَضَعْنَ حَمْلَهُنَّ ۚ
فَاِنْ اَرْضَعْنَ لَكُمْ فَاٰتُوْهُنَّ اُجُوْرَهُنَّ ۚ
وَاْتَمِرُوْا بَيْنَكُمْ بِمَعْرُوْفٍ ۚ وَاِنْ
تَعَاسَرْتُمْ فَسَتُرْضِعُ لَهٗۤ اُخْرٰى ۝٦

7. Wawekeni humo humo mnamokaa ninyi, sawa na hali zenu, wala msiwadhuru kwa kuwatia katika dhiki; na kama wakiwa na mimba, basi wagharamieni mpaka wajifungue. Na kama wakiwanyonyesheeni, basi wapeni ujira wao, na shaurianeni kwa wema, na kama mkiona udhia baina yenu, basi amnyonyeshee (mwanamke) mwingine.

لِيُنْفِقْ ذُوْ سَعَةٍ مِّنْ سَعَتِهٖ ؕ وَمَنْ قُدِرَ
عَلَيْهِ رِزْقُهٗ فَلْيُنْفِقْ مِمَّاۤ اٰتٰىهُ اللّٰهُ ؕ لَا
يُكَلِّفُ اللّٰهُ نَفْسًا اِلَّا مَاۤ اٰتٰىهَا ؕ سَيَجْعَلُ
اللّٰهُ بَعْدَ عُسْرٍ يُّسْرًا ۝٧

8. Mwenye wasaa agharimie kadiri ya wasaa wake, na yule ambaye amepungukiwa riziki yake, basi atoe katika kile Alichompa Allah; Allah hamkalifishi mtu ye yote ila kwa kadiri Alivyompa; karibuni Allah Atamfariji baada ya shida. ع

FUNGU 2

وَكَاَيِّنْ مِّنْ قَرْيَةٍ عَتَتْ عَنْ اَمْرِ رَبِّهَا
وَرُسُلِهٖ فَحَاسَبْنٰهَا حِسَابًا شَدِيْدًا ۙ
وَّعَذَّبْنٰهَا عَذَابًا نُّكْرًا ۝٨

9. Na miji mingapi iliyovunja amri ya Mola wao na Mitume Wake, basi Tuliihesabia hesabu ngumu na Tukaiadhibu kwa adhabu kali.

فَذَاقَتْ وَبَالَ اَمْرِهَا وَكَانَ عَاقِبَةُ
اَمْرِهَا خُسْرًا ۝٩

10. Basi ikauonja ubaya wa mambo yao, na mwisho wa mambo yao ukawa ni hasara.

اَعَدَّ اللّٰهُ لَهُمْ عَذَابًا شَدِيْدًا ۙ فَاتَّقُوا اللّٰهَ
يٰۤاُولِي الْاَلْبَابِ ۚ الَّذِيْنَ اٰمَنُوْا ۛ
قَدْ اَنْزَلَ اللّٰهُ اِلَيْكُمْ ذِكْرًا ۝١٠

11. Allah Akawaandalia adhabu kali, basi Mcheni Allah, enyi wenye akili, mlioamini, hakika Allah Amewateremshieni Ukumbusho

رَّسُوْلًا يَّتْلُوْا عَلَيْكُمْ اٰيٰتِ اللّٰهِ مُبَيِّنٰتٍ
لِّيُخْرِجَ الَّذِيْنَ اٰمَنُوْا وَعَمِلُوا الصّٰلِحٰتِ
مِنَ الظُّلُمٰتِ اِلَى النُّوْرِ ؕ وَمَنْ يُّؤْمِنْ

12. Mtume anayewasomeeni Aya za Allah zinazobainisha, ili kuwatoa wale walioamini na watendao mema katika giza kuwapeleka kwenye

بِاللّٰهِ وَيَعْمَلْ صَالِحًا يُّدْخِلْهُ جَنّٰتٍ تَجْرِيْ مِنْ تَحْتِهَا الْاَنْهٰرُ خٰلِدِيْنَ فِيْهَآ اَبَدًا ؕ قَدْ اَحْسَنَ اللّٰهُ لَهٗ رِزْقًا ⑪

nuru; na anayemwamini Allah na kutenda mema Atamwingiza katika Pepo zipitazo mito ndani yake, watakaa humo milele. Bila shaka Allah Amekwisha mpa riziki nzuri.

اَللّٰهُ الَّذِيْ خَلَقَ سَبْعَ سَمٰوٰتٍ وَّمِنَ الْاَرْضِ مِثْلَهُنَّ ؕ يَتَنَزَّلُ الْاَمْرُ بَيْنَهُنَّ لِتَعْلَمُوْٓا اَنَّ اللّٰهَ عَلٰى كُلِّ شَيْءٍ قَدِيْرٌ ۙ وَّاَنَّ اللّٰهَ قَدْ اَحَاطَ بِكُلِّ شَيْءٍ عِلْمًا ⑫ ع

13. Allah ni Yule Ambaye Amezi-umba mbingu saba, na ardhi mfano wa hizo. Amri zinashuka katikati yao, ili mjue kwamba Allah ni Mwenye uwezo juu ya kila kitu, na kwamba Allah Amekizunguka kila kitu kwa elimu.

سُوْرَةُ التَّحْرِيْمِ مَدَنِيَّةٌ وَّ هِيَ مَعَ الْبَسْمَلَةِ ثَلَاثَ عَشْرَةَ اٰيَةً وَّ رُكُوْعَانِ

66. SURA AT-TAHRIIM

Imeteremshwa Madina

Ina mafungu 2 na Aya 13 pamoja na Bismillahi

بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ ①

1. Kwa jina la Allah, Mwingi wa rehema, Mwingi wa ukarimu.

يٰۤاَيُّهَا النَّبِيُّ لِمَ تُحَرِّمُ مَاۤ اَحَلَّ اللّٰهُ لَكَ ۚ تَبْتَغِيْ مَرْضَاتَ اَزْوَاجِكَ ؕ وَاللّٰهُ غَفُوْرٌ رَّحِيْمٌ ②

2. Ewe Nabii! mbona unaharamisha Alichokuhalalishia Allah? Unatafuta radhi ya wake zako; na Allah ni Msamehevu, Mwingi wa Ukarimu.

قَدْ فَرَضَ اللّٰهُ لَكُمْ تَحِلَّةَ اَيْمَانِكُمْ ۚ وَاللّٰهُ مَوْلٰىكُمْ ۚ وَهُوَ الْعَلِيْمُ الْحَكِيْمُ ③

3. Hakika Allah Kawalazimisheni mfungue viapo vyenu, na Allah ni Mlinzi wenu; naye Ndiye Ajuaye kila kitu, Mwenye hekima.

وَاِذْ اَسَرَّ النَّبِيُّ اِلٰى بَعْضِ اَزْوَاجِهٖ حَدِيْثًا ۚ فَلَمَّا نَبَّاَتْ بِهٖ وَاَظْهَرَهُ اللّٰهُ عَلَيْهِ عَرَّفَ بَعْضَهٗ وَاَعْرَضَ عَنْۢ

4. Na Nabii alipomwambia mmoja wa wake zake hadithi kwa siri, basi (mke yule) alipoivunja siri, na Allah Akamdhihirishia (Nabii), akajulisha sehemu yake na akaacha sehemu nyingine. Basi alipompasha

---

Sura hii imeitwa *Kuharimisha* kwa ajili ya neno lililotumiwa katika Aya 2 inayokataza ya kuwa Mtume asijiharimishie vitu alivyohalalisha Allah.

Sura hii ilishuka Madina, yumkini katika mwaka wa 7 wa Hijra.

Aya 2. *Mbona unaharimisha.* Mtume alijiharimishia asali kwa sababu harufu yake iliwaudhi baadhi ya wakeze. Mtume akaona, 'kama tusitumie asali kuna ubaya gani?' Akaacha kuitumia. Jambo hili lingeleta taabu kwa Waislamu ambao wangefuata mwendo huo wa Mtume *s.a.w.* kuwa sunna. Basi Allah akamkataza katika Aya hii (Bukhari na Muslim).

Kadhalika Mtume *s.a.w.* aliudhiwa na wakeze juu ya jambo fulani basi akajitenga nao kwa muda wa mwezi mmoja; jambo hili pia limekatazwa hapa isije Waislamu wakalifuata kama sunna, (Bukhari na Muslim).

Aya 4. *Hadithi kwa siri.* Shia wanasema hadithi ya siri ilikuwa ya kwamba Seyidna Ali ndiye atakuwa Khalifa baada ya Mtume. Sunni wanasema hadithi hii ni kuwa Seyidna Abu Bakar

(mkewe) habari hii akasema: Nani amekupa habari hii? (Nabii) akasema: Amenipa habari Aliye ni Mjuzi, Mwenye habari.

بَعْضٍ ۚ فَلَمَّا نَبَّاَهَا بِهٖ قَالَتْ مَنْ اَنْۢبَاَكَ هٰذَا ؕ قَالَ نَبَّاَنِيَ الْعَلِيْمُ الْخَبِيْرُ ۝

5. Kama ninyi wawili mtatubu kwa Allah, basi mioyo yenu imekwisha elekea, na kama mtasaidiana juu yake, basi Allah ndiye Mlinzi wake, na Jibril, na waaminio wema, na zaidi ya hayo (pia) Malaika ni wasaidizi (wake).

اِنْ تَتُوْبَاۤ اِلَى اللّٰهِ فَقَدْ صَغَتْ قُلُوْبُكُمَا ۚ وَاِنْ تَظٰهَرَا عَلَيْهِ فَاِنَّ اللّٰهَ هُوَ مَوْلٰىهُ وَجِبْرِيْلُ وَصَالِحُ الْمُؤْمِنِيْنَ ۚ وَالْمَلٰٓئِكَةُ بَعْدَ ذٰلِكَ ظَهِيْرٌ ۝

---

na Umar watakuwa Makhalifa baada yake; na Padre Dale naye ameokota hadithi hii na kutafuta kuleta aibu juu ya Mtume. Lakini je, siri hiyo ambayo Allah Mwenyewe hakuitaja watu wana haki gani ya kubuni hadithi yao wenyewe na kusema ndiyo siri hiyo?

Wakristo na Mabaniani wameleta upinzani juu ya Aya za kwanza za sura hii. Wanasema, Hafsa, mkewe Mtume s.a.w. alikuwa na mjakazi aitwaye Maria Kibtiyya. Akamkuta Mtume anaingiliana na mjakazi huyu, na akakasirika. Mtume kutaka kuficha siri ile na uvumi usienee akamwambia Hafsa kuwa hataingiliana na mjakazi yule tena, na baba yake atakuwa Khalifa baada yake, basi asitoe siri ile. Lakini Hafsa akamwambia Aisha habari ile na Aisha akamwulizayo Mtume. Basi Mtume akateremshiwa Aya ya kutoa ruhusa kuvunja kiapo.

1. Jambo la kwanza, hadithi hii hakuna katika Qur'an wala katika Hadithi. Labda watasema wameipata kwa waliofasiri Qur'an, lakini hata Wakristo kama Sale na Dale na wengineo wameifasiri Qur'an. Je, tutamlaumu Mtume wa Mungu kwa maneno yanayotungwa na wanaofasiri? Kila mtu anaweza kujitungia apendavyo. Watuletee ushahidi wa habari hii katika Qur'an au Hadithi ikiwa wanasema kweli. Lakini kamwe hawatapata.

2. Maneno ya Padre Dale yanaonyesha kuwa Maria Kibtiyya alikuwa mkewe Mtume s.a.w. na alikuwa na zamu kama wakeze wengine. Maneno haya yanapinzana na ya Mapadre wenzake wanaodai kuwa Maria alikuwa ni mjakazi wa Hafsa na kusema (Mungu apishe mbali) kuwa Mtume alizini naye, kisha akaapa na akavunja kiapo, na zaidi ya hayo akaendelea kuingiliana naye. Uwongo wao unaanza kufichuana.

3. Maria Kibtiyya hakuwa mjakazi wa Hafsa kama wanavyoshuku hawa, bali yeye aliletwa zawadi pamoja na nyumbu kwa Mtume toka kwa mfalme wa Kikristo aitwaye Mukaukas aliyekuwa anatawala Misri na Alexandria. Na mwanamke huyu alizaa na Mtume mtoto aitwaye Ibrahimu ambaye alifariki bado mchanga. Sasa ni wazi kabisa mashtaka haya yote ya Wakristo na Mabaniani yanavunjika kwa kuthibitika kuwa Maria hakuwa mjakazi wa Hafsa.

4. Ama wale wanaosema ya kuwa Mtume *s.a.w.* ilikuwa desturi yake kuteremsha Aya ili zimsaidie katika yale anayoyapenda kufanya wanasema uwongo kabisa.

(i) Katika vita ya Tabuk wanafiki waliomba ruhusa kukaa nyuma na Mtume *s.a.w.* akawapa. Allah anamwambia kwa nini aliwapa ruhusa kabla hajapambanua nani mkweli na nani mwongo (sura 9:44).

(ii) Mtume *s.a.w.* alisalia jeneza ya mnafiki mmoja aitwaye Abdullah bin Ubayy bin Salul akifikiri kuwa hakuna ubaya akifanya hivyo. lakini Allah akamkataza baadaye asisalie wanafiki (sura 9:85).

عَسٰى رَبُّهٗۤ اِنۡ طَلَّقَكُنَّ اَنۡ يُّبۡدِلَهٗۤ اَزۡوَاجًا خَيۡرًا مِّنۡكُنَّ مُسۡلِمٰتٍ مُّؤۡمِنٰتٍ قٰنِتٰتٍ تٰٓئِبٰتٍ عٰبِدٰتٍ سٰٓئِحٰتٍ ثَيِّبٰتٍ وَّاَبۡكَارًا ۝٥

6. (Nabii) akiwapeni talaka, yumkini Mola wake Atamletea badala yenu wake wengine walio bora kuliko ninyi, waliosilimu, waaminio, watii sana, watubiao, wafanyao ibada, wafungao saumu, wajane na mabikira.

يٰۤاَيُّهَا الَّذِيۡنَ اٰمَنُوۡا قُوۡۤا اَنۡفُسَكُمۡ وَاَهۡلِيۡكُمۡ نَارًا وَّقُوۡدُهَا النَّاسُ وَالۡحِجَارَةُ عَلَيۡهَا مَلٰٓئِكَةٌ غِلَاظٌ شِدَادٌ لَّا يَعۡصُوۡنَ اللّٰهَ مَاۤ اَمَرَهُمۡ وَيَفۡعَلُوۡنَ مَا يُؤۡمَرُوۡنَ ۝٦

7. Enyi mlioamini! Jiokoeni nafsi zenu na ahali zenu katika Moto ambao kuni zake ni watu na mawe; juu yake wako Malaika wakali, wenye nguvu, hawamwasi Allah Aliyowaamuru, na hutenda wanayoamrishwa.

يٰۤاَيُّهَا الَّذِيۡنَ كَفَرُوۡا لَا تَعۡتَذِرُوا الۡيَوۡمَ ؕ اِنَّمَا تُجۡزَوۡنَ مَا كُنۡتُمۡ تَعۡمَلُوۡنَ ۝٧ ع ١٩

8. Enyi mliokufuru! msilete udhuru leo; bila shaka mtapewa malipo ya yale mliyokuwa mkitenda.

FUNGU 2

يٰۤاَيُّهَا الَّذِيۡنَ اٰمَنُوۡا تُوۡبُوۡۤا اِلَى اللّٰهِ تَوۡبَةً نَّصُوۡحًا ؕ عَسٰى رَبُّكُمۡ اَنۡ يُّكَفِّرَ عَنۡكُمۡ سَيِّاٰتِكُمۡ وَيُدۡخِلَكُمۡ جَنّٰتٍ تَجۡرِىۡ مِنۡ تَحۡتِهَا الۡاَنۡهٰرُ ۙ يَوۡمَ لَا يُخۡزِى اللّٰهُ النَّبِىَّ وَالَّذِيۡنَ اٰمَنُوۡا مَعَهٗ ۚ نُوۡرُهُمۡ يَسۡعٰى بَيۡنَ اَيۡدِيۡهِمۡ وَبِاَيۡمَانِهِمۡ يَقُوۡلُوۡنَ رَبَّنَاۤ اَتۡمِمۡ لَنَا نُوۡرَنَا وَاغۡفِرۡ لَنَا ۚ اِنَّكَ عَلٰى كُلِّ شَىۡءٍ قَدِيۡرٌ ۝٨

9. Enyi mlioamini! Tubuni kwa Allah toba iliyotakasika; huenda Mola wenu Akawafutieni maovu yenu na kuwaingizeni katika Pepo zipitazo mito ndani yake, siku ambayo Allah Hatamfedhehesha Nabii na wale walioamini pamoja naye; nuru yao itapiga mbio mbele yao na upande wa mikono yao ya kuume; watasema: Mola wetu, Ututimizie nuru yetu, na Utughofirie; hakika Wewe ni Mwenye uwezo juu ya kila kitu.

يٰۤاَيُّهَا النَّبِىُّ جَاهِدِ الۡكُفَّارَ وَالۡمُنٰفِقِيۡنَ وَاغۡلُظۡ عَلَيۡهِمۡ ؕ وَمَاۡوٰىهُمۡ جَهَنَّمُ ؕ وَبِئۡسَ الۡمَصِيۡرُ ۝٩

10. Ewe Nabii! shindana na makafiri na wanafiki na uwe mgumu kwao; na kimbilio lao ni Jahanamu, nayo ni marejeo mabaya.

ضَرَبَ اللّٰهُ مَثَلًا لِّلَّذِيْنَ كَفَرُوا امْرَاَتَ نُوْحٍ وَّامْرَاَتَ لُوْطٍ ؕ كَانَتَا تَحْتَ عَبْدَيْنِ مِنْ عِبَادِنَا صَالِحَيْنِ فَخَانَتٰهُمَا فَلَمْ يُغْنِيَا عَنْهُمَا مِنَ اللّٰهِ شَيْـًٔا وَّ قِيْلَ ادْخُلَا النَّارَ مَعَ الدّٰخِلِيْنَ ﴿۱۰﴾

11. Allah Amepiga mfano wa waliokufuru kwa mkewe Nuhu na mkewe Luti: hawa wawili walikuwa chini ya Watumishi wema wawili miongoni mwa Watumishi Wetu, basi (wanawake hao) wakawafanyia hiyana, (lakini waume zao) hawakuwasaidia cho chote mbele ya Allah, na ikasemwa: Uingieni Moto pamoja na waingiao.

وَضَرَبَ اللّٰهُ مَثَلًا لِّلَّذِيْنَ اٰمَنُوا امْرَاَتَ فِرْعَوْنَ ۘ اِذْ قَالَتْ رَبِّ ابْنِ لِيْ عِنْدَكَ بَيْتًا فِي الْجَنَّةِ وَنَجِّنِيْ مِنْ فِرْعَوْنَ وَعَمَلِهٖ وَنَجِّنِيْ مِنَ الْقَوْمِ الظّٰلِمِيْنَ ﴿۱۱﴾

12. Na (tena) Allah Amepiga mfano wa walioamini kwa mkewe Firauni, عليه السلام aliposema: Ee Mola wangu, Unijengee nyumba Peponi karibu Yako, na Uniokoe na Firauni na matendo yake, na Uniokoe katika watu wadhalimu.

وَمَرْيَمَ ابْنَتَ عِمْرٰنَ الَّتِيْٓ اَحْصَنَتْ فَرْجَهَا فَنَفَخْنَا فِيْهِ مِنْ رُّوْحِنَا وَصَدَّقَتْ بِكَلِمٰتِ رَبِّهَا وَكُتُبِهٖ وَكَانَتْ مِنَ الْقٰنِتِيْنَ ﴿۱۲﴾ ع

13. Na (mfano wa) Mariamu binti Imrani aliyeilinda heshima yake, na Tukapulizia ndani yake (mtoto yule) roho Yetu na akayasadikisha maneno ya Mola wake, na Vitabu Vyake; na alikuwa miongoni mwa wanyenyekevu.

Aya 12-13. Katika Aya hizi wametajwa waaminio namna mbili: (1) watu kama mke wa Firauni ambaye alikuwa mwenye kuamini, na akaficha imani yake na akachukia mambo ya Firauni, na akamwomba Mungu amwokoe na Firauni na (2) watu kama Mariamu mama wa Nabii Isa, ambao wanaomaliza maisha yao kwa ajili ya Allah na wanapuliziwa roho takatifu inayowaimarisha kuendesha mapendeleo ya Allah na wanakuwa sawasawa na Masihi, na hawajali watu wanasema nini katika kazi yao ya kutangaza haki.

سُوْرَةُ الْمُلْكِ مَكِّيَّةٌ وَّ هِيَ مَعَ الْبَسْمَلَةِ اِحْدٰى وَ ثَلَاثُوْنَ اٰيَةً وَّ رُكُوْعَانِ

67. SURA AL-MULK

Imeteremshwa Makka

Ina mafungu 2 na Aya 31 pamoja na Bismillahi

JUZU 29

بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ ①

1. Kwa jina la Allah, Mwingi wa rehema, Mwingi wa ukarimu.

تَبٰرَكَ الَّذِيْ بِيَدِهِ الْمُلْكُ ۖ وَهُوَ عَلٰى كُلِّ شَيْءٍ قَدِيْرُ ۙ ②

2. Mwenye baraka ni Yule tu Ambaye Mkononi Mwake umo ufalme, naye ni Mwenye uwezo juu ya kila kitu,

الَّذِيْ خَلَقَ الْمَوْتَ وَالْحَيٰوةَ لِيَبْلُوَكُمْ اَيُّكُمْ اَحْسَنُ عَمَلًا ۭ وَهُوَ الْعَزِيْزُ الْغَفُوْرُ ۙ ③

3. Ambaye Aliumba kifo na uhai ili kuwajaribuni, ni nani miongoni mwenu aliye mbora kwa vitendo; naye ni Mwenye ushindi kamili, Mwenye kusamehe;

الَّذِيْ خَلَقَ سَبْعَ سَمٰوٰتٍ طِبَاقًا ۭ مَا تَرٰى فِيْ خَلْقِ الرَّحْمٰنِ مِنْ تَفٰوُتٍ ۭ فَارْجِعِ الْبَصَرَ ۙ هَلْ تَرٰى مِنْ فُطُوْرٍ ④

4. Ambaye Aliumba mbingu saba zilizo tabaka-tabaka, huoni tofauti yo yote katika uumbaji wa Rahmani; basi rudisha macho, je unaona kosa?

ثُمَّ ارْجِعِ الْبَصَرَ كَرَّتَيْنِ يَنْقَلِبْ اِلَيْكَ الْبَصَرُ خَاسِئًا وَّهُوَ حَسِيْرٌ ⑤

5. Tena rudisha macho mara ya pili; mtazamo wako utakurudia katika hali ya kutofanikiwa na ya mchoko.

وَلَقَدْ زَيَّنَّا السَّمَآءَ الدُّنْيَا بِمَصَابِيْحَ وَجَعَلْنٰهَا رُجُوْمًا لِّلشَّيٰطِيْنِ وَاَعْتَدْنَا لَهُمْ عَذَابَ السَّعِيْرِ ⑥

6. Na kwa hakika Tumeipamba mbingu ya karibu kwa mataa, na Tumeyafanya ili kuwapiga mashetani, na Tumewawekea tayari adhabu ya moto uwakao.

Jina la sura hii linatokea katika maneno yaliyomo katika Aya ya 2 ya kuwa ufalme umo mikononi mwa Allah. Sura hii ilishuka Makka.

Aya 3. *'Aziiz,* "Mwenye heshima." Neno hili pia maana yake ni Mwenye nguvu na Mwenye ushindi kamili.

Aya 5. *Tena rudisha macho.* Maana yake, pelelezeni sana kazi iliyofanywa na Allah na chungueni na fikirini na endeleeni kutazama na kuangalia, lakini juu ya hayo hamtakuta upungufu au kasoro katika kazi Yake. Mwisho mtachoka tu katika upelelezi wenu bila kuona kosa lo lote katika uumbaji wa Allah.

وَلِلَّذِيْنَ كَفَرُوْا بِرَبِّهِمْ عَذَابُ جَهَنَّمَ ؕ وَبِئْسَ الْمَصِيْرُ ۝٧

7. Na kwa waliomkufuru Mola wao iko adhabu ya Jahanamu; na ni marejeo mabaya yaliyoje!

اِذَآ اُلْقُوْا فِيْهَا سَمِعُوْا لَهَا شَهِيْقًا وَّهِيَ تَفُوْرُ ۙ ۝٨

8. Watakapotupwa humo watasikia rindimo lake nao utafura,

تَكَادُ تَمَيَّزُ مِنَ الْغَيْظِ ؕ كُلَّمَآ اُلْقِيَ فِيْهَا فَوْجٌ سَاَلَهُمْ خَزَنَتُهَآ اَلَمْ يَاْتِكُمْ نَذِيْرٌ ۝٩

9. Karibu upasuke kwa hasira. Kila mara litakapotupwa humo kundi walinzi wake watawauliza: Je, hakuwafikieni Mwonyaji?

قَالُوْا بَلٰى قَدْ جَآءَنَا نَذِيْرٌ ۙ فَكَذَّبْنَا وَقُلْنَا مَا نَزَّلَ اللّٰهُ مِنْ شَيْءٍ ۖ اِنْ اَنْتُمْ اِلَّا فِيْ ضَلٰلٍ كَبِيْرٍ ۝١٠

10. Watasema: Naam! Alitufikia Mwonyaji, lakini tulikadhibisha na tulisema: Allah Hakuteremsha cho chote, ninyi hammo ila katika upotevu mkubwa.

وَقَالُوْا لَوْ كُنَّا نَسْمَعُ اَوْ نَعْقِلُ مَا كُنَّا فِيْٓ اَصْحٰبِ السَّعِيْرِ ۝١١

11. Na watasema: Kama tungalikuwa tunasikia au tungalikuwa na akili hatungekuwa katika watu wa Motoni.

فَاعْتَرَفُوْا بِذَنْۢبِهِمْ ۚ فَسُحْقًا لِّاَصْحٰبِ السَّعِيْرِ ۝١٢

12. Kisha wakakiri dhambi zao; basi ni maangamio kwa watu wa Motoni.

اِنَّ الَّذِيْنَ يَخْشَوْنَ رَبَّهُمْ بِالْغَيْبِ لَهُمْ مَّغْفِرَةٌ وَّاَجْرٌ كَبِيْرٌ ۝١٣

13. Hakika wale wanaomwogopa Mola wao Akiwa Amefichika machoni pao, wao watapata msamaha na malipo makubwa.

وَاَسِرُّوْا قَوْلَكُمْ اَوِ اجْهَرُوْا بِهٖ ؕ اِنَّهٗ عَلِيْمٌۢ بِذَاتِ الصُّدُوْرِ ۝١٤

14. Na ificheni kauli yenu au idhihirisheni; hakika Yeye ni Mjuzi wa yaliyomo vifuani.

اَلَا يَعْلَمُ مَنْ خَلَقَ ؕ وَهُوَ اللَّطِيْفُ الْخَبِيْرُ ۝١٥ ع

15. Je, Yeye Aliyeumba Hajui? Naye ndiye Aonaye visivyoonekana, Mwenye habari.

FUNGU 2

هُوَ الَّذِيْ جَعَلَ لَكُمُ الْاَرْضَ ذَلُوْلًا فَامْشُوْا فِيْ مَنَاكِبِهَا وَكُلُوْا مِنْ رِّزْقِهٖ ؕ وَاِلَيْهِ النُّشُوْرُ ۝١٦

16. Yeye ndiye Aliyeifanya ardhi mororo kwa ajili yenu; basi tembeeni katika pande zake na kuleni katika riziki Zake, na Kwake ni ufufuo.

Aya 16. *Dhaluulan,* "mororo." Neno hili pia lina maana ya "ardhi iliyowekwa chini ya

ءَاَمِنْتُمْ مَّنْ فِي السَّمَآءِ اَنْ يَّخْسِفَ بِكُمُ الْاَرْضَ فَاِذَا هِيَ تَمُوْرُ ﴿١٧﴾

17. Je, mmesalimika na Yule Aliyeko mbinguni ya kuwa Yeye Hatawadidimizeni ardhini, basi nayo ghafla inatetemeka?

اَمْ اَمِنْتُمْ مَّنْ فِي السَّمَآءِ اَنْ يُّرْسِلَ عَلَيْكُمْ حَاصِبًا ؕ فَسَتَعْلَمُوْنَ كَيْفَ نَذِيْرِ ﴿١٨﴾

18. Au je! mmesalimika na Aliyeko mbinguni ya kuwa Yeye Hatawapelekeeni kimbunga chenye changarawe? Basi karibuni mtajua onyo Langu lilikuwaje.

وَلَقَدْ كَذَّبَ الَّذِيْنَ مِنْ قَبْلِهِمْ فَكَيْفَ كَانَ نَكِيْرِ ﴿١٩﴾

19. Na bila shaka wamekwisha kadhibisha wale wa kabla yao, basi adhabu yangu ilikuwa kali kiasi gani?

اَوَلَمْ يَرَوْا اِلَى الطَّيْرِ فَوْقَهُمْ صٰٓفّٰتٍ وَّيَقْبِضْنَ ۛ مَا يُمْسِكُهُنَّ اِلَّا الرَّحْمٰنُ ؕ اِنَّهٗ بِكُلِّ شَيْءٍۭ بَصِيْرٌ ﴿٢٠﴾

20. Je, hawaangalii ndege walioko juu yao wakizinyosha (mbawa zao) na kuzikunja? Hakuna Awashikiliaye ila Mungu wa huruma. Hakika Yeye Anaona kila kitu.

اَمَّنْ هٰذَا الَّذِيْ هُوَ جُنْدٌ لَّكُمْ يَنْصُرُكُمْ مِّنْ دُوْنِ الرَّحْمٰنِ ؕ اِنِ الْكٰفِرُوْنَ اِلَّا فِيْ غُرُوْرٍ ﴿٢١﴾

21. Au ni nani hao walio jeshi lenu wawezao kuwasaidieni pasipo Rahman? Hawako makafiri ila katika udanganyifu.

اَمَّنْ هٰذَا الَّذِيْ يَرْزُقُكُمْ اِنْ اَمْسَكَ رِزْقَهٗ ۚ بَلْ لَّجُّوْا فِيْ عُتُوٍّ وَّنُفُوْرٍ ﴿٢٢﴾

22. Au ni nani ambaye atawapeni riziki kama Akizizuia riziki Zake? Bali wanaendelea tu katika uasi na chuki.

اَفَمَنْ يَّمْشِيْ مُكِبًّا عَلٰى وَجْهِهٖٓ اَهْدٰٓى اَمَّنْ يَّمْشِيْ سَوِيًّا عَلٰى صِرَاطٍ مُّسْتَقِيْمٍ ﴿٢٣﴾

23. Je, anayekwenda kifudifudi kwa uso wake ni mwongofu zaidi au anayekwenda sawasawa katika njia iliyonyoka?

قُلْ هُوَ الَّذِيْٓ اَنْشَاَكُمْ وَجَعَلَ لَكُمُ السَّمْعَ وَالْاَبْصَارَ وَالْاَفْـِٕدَةَ ؕ قَلِيْلًا مَّا تَشْكُرُوْنَ ﴿٢٤﴾

24. Sema: Yeye ndiye Aliyewaumbeni na Akawapeni masikio na macho na mioyo; ni kidogo tu mnayoshukuru.

---

mamlaka yenu kwa urahisi."

Tembeeni katika pande zake, yaani kama mahali pamoja hapawafaeni nendeni upande au mahali pengine ; na kama watu hawasikii ubashiri wenu mahali pamoja ondokeni mkahubiri mahali pengine.

Aya 22. *Akizuia riziki Zake.* Ubashiri huu ulitimia ilipotokea njaa ya miaka saba katika Makka na shida kubwa iliwafikia watu hata walikuwa wakisaga mifupa kufanya chakula.

قُلْ هُوَ الَّذِیْ ذَرَاَكُمْ فِی الْاَرْضِ وَاِلَیْهِ تُحْشَرُوْنَ ﴿۲۵﴾

25. Sema: Yeye ndiye Aliyewaumbeni ardhini na Kwake mtakusanywa.

وَیَقُوْلُوْنَ مَتٰی هٰذَا الْوَعْدُ اِنْ كُنْتُمْ صٰدِقِیْنَ ﴿۲۶﴾

26. Nao husema: Lini (itatimizwa) ahadi hii ikiwa mnasema kweli?

قُلْ اِنَّمَا الْعِلْمُ عِنْدَ اللّٰهِ ۫ وَاِنَّمَاۤ اَنَا نَذِیْرٌ مُّبِیْنٌ ﴿۲۷﴾

27. Sema: Kwa kweli elimu iko kwa Allah, na hakika mimi ni Mwonyaji tu nibainishaye.

فَلَمَّا رَاَوْهُ زُلْفَةً سِیْٓـَٔتْ وُجُوْهُ الَّذِیْنَ كَفَرُوْا وَقِیْلَ هٰذَا الَّذِیْ كُنْتُمْ بِهٖ تَدَّعُوْنَ ﴿۲۸﴾

28. Lakini watakapoiona karibu, nyuso za waliokufuru zitahuzunika, na itasemwa: Hayo ndiyo mliyokuwa mkiyaomba.

قُلْ اَرَءَیْتُمْ اِنْ اَهْلَكَنِیَ اللّٰهُ وَمَنْ مَّعِیَ اَوْ رَحِمَنَا ۙ فَمَنْ یُّجِیْرُ الْكٰفِرِیْنَ مِنْ عَذَابٍ اَلِیْمٍ ﴿۲۹﴾

29. Sema: Niambieni kama Allah Akiniangamiza mimi na walio pamoja nami, au Akiturehemu, basi ni nani atakayewalinda makafiri na adhabu iumizayo?

قُلْ هُوَ الرَّحْمٰنُ اٰمَنَّا بِهٖ وَعَلَیْهِ تَوَكَّلْنَا ۚ فَسَتَعْلَمُوْنَ مَنْ هُوَ فِیْ ضَلٰلٍ مُّبِیْنٍ ﴿۳۰﴾

30. Sema: ni Yeye Ndiye Mwingi wa rehema, tunamwamini Yeye, na Kwake tunategemea, na karibuni mtajua ni nani aliye katika upotevu dhahiri.

قُلْ اَرَءَیْتُمْ اِنْ اَصْبَحَ مَآؤُكُمْ غَوْرًا فَمَنْ یَّاْتِیْكُمْ بِمَآءٍ مَّعِیْنٍ ﴿۳۱﴾ ع ۲

31. Sema: Niambieni, kama maji yenu yakizama chini kabisa, ni nani basi atakayekuleteeni maji ya chemchemu?

Aya 25. *Dhara'akum,* neno hili tumelifasiri, "aliyewaongozeni." Pia maana yake' "aliyewaumbeni."

Aya 27. *Innamaa,* tumelifasiri, "kwa kweli" kwa mujibu wa mchukuzano wa usemi mzuri wa Kiswahili, nalo lina maana ya "hakika," "hasa," "kwa yakini," n.k.w. ambayo ni maneno yatiayo mkazo kama tulivyofasiri.

سُوْرَةُ الْقَلَمِ مَكِّيَّةٌ وَّ هِيَ مَعَ الْبَسْمَلَةِ ثَلَاثٌ وَّ خَمْسُوْنَ اٰيَةً وَّ رُكُوْعَانِ

68. SURA AL-QALAM

Imeteremshwa Makka

Ina mafungu 2 na Aya 53 pamoja na Bismillahi

بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ ①

1. Kwa jina la Allah, Mwingi wa rehema, Mwingi wa ukarimu.

نٓ وَالْقَلَمِ وَمَا يَسْطُرُوْنَ ②

2. (Naapa kwa) kidau na kalamu na yale wayaandikayo,

مَآ اَنْتَ بِنِعْمَةِ رَبِّكَ بِمَجْنُوْنٍ ③

3. Kwa neema ya Mola wako wewe si majnuni.

وَ اِنَّ لَكَ لَاَجْرًا غَيْرَ مَمْنُوْنٍ ④

4. Na kwa hakika una malipo yasiyokatizwa.

وَ اِنَّكَ لَعَلٰى خُلُقٍ عَظِيْمٍ ⑤

5. Na bila shaka una tabia njema, tukufu.

Mtume *s.a.w.* alipotangaza ujumbe wake, kwanza wasioamini walimwita mwehu, na sura hii mwanzoni inatoa jawabu la upinzani huo. Kidau na kalamu na vinavyoandikwa vinatolewa viwe ushahidi wa kwamba Mtume s.a.w. si mwehu. Katika jambo hili sura hii imeitwa *Qalam* yaani "Kalamu."

Wanazuoni wanaifahamu sura hii kuwa ilishuka mwanzoni sana hata inafahamiwa kuwa ni ya pili katika kushuka kwa Qur'an. Lakini kwa kuwa sura ya 74 inaonyeshwa na Hadithi zilizo sahihi kuwa ndiyo ya kwanza, basi sura hii itakuwa ni baada ya hiyo, nayo ilishuka Makka.

Aya 3. *Wewe si majnuni.* Upinzani wa kwanza ulioletwa na makafiri juu ya Mtume *s.a.w.* ni kwamba yeye ni mwehu. Na upinzani huu unajibiwa katika Aya ya kwanza Allah anapoapa kwa kidau na kalamu na yanayoandikwa. Yaani, elimu zote zitakazoandikwa duniani hazitakuwa na uwezo wa kuhakikisha kuwa Qur'an ina makosa na hii itadhihirisha daima kuwa aliyeleta Qur'an si mtu majnuni.

Aya 4. *Malipo yasiyokatizwa.* Kama Mtume *s.a.w.* angekuwa majnuni kazi yake ingekuwa ovyo na isingeleta matokeo yo yote. Upande mmoja maadui zake walisimama kumpinga naye alisimama imara kuendesha kazi yake; na maadui zake walishindwa na kazi ya Mtume s.a.w. inaendelea siku zote, hali maadui zake wamebakia na jina baya tu. Hii inaonyesha dhahiri kabisa malipo anayopata Mtume hayana mwisho, kwa vile mafaniko yake yanazidi kuendelea kila siku.

Aya 5. *Una tabia njema, tukufu.* Hii ni dalili nyingine ya kuwa Mtume *s.a.w.* hakuwa majnuni. Makafiri wenyewe walikiri kuwa yeye alikuwa mwaminifu sana na mkweli. Sasa majnuni hawezi kuwa na sifa za namna hii. Mkewe Aisha alipoulizwa juu ya tabia za Mtume *s.a.w.* alisema kuwa tabia zake ni hizo hizo zinazoelezwa katika Qur'an. Basi mtu mwenye tabia njema za namna hii kumwita mwehu si ulalamishi wa bure?

فَسَتُبۡصِرُ وَيُبۡصِرُوۡنَ ۙ﴿۶﴾

6. Basi karibuni utaona, nao pia wataona,

بِاَيِّيۡكُمُ الۡمَفۡتُوۡنُ ﴿۷﴾

7. Ni nani mwenye kichaa miongoni mwenu.

اِنَّ رَبَّكَ هُوَ اَعۡلَمُ بِمَنۡ ضَلَّ عَنۡ سَبِيۡلِهٖ ۖ وَهُوَ اَعۡلَمُ بِالۡمُهۡتَدِيۡنَ ﴿۸﴾

8. Hakika Mola wako Anamjua sana aliyepotea katika njia Yake na Yeye Anawajua sana walioongoka.

فَلَا تُطِعِ الۡمُكَذِّبِيۡنَ ﴿۹﴾

9. Basi usiwatii wanaokadhibisha.

وَدُّوۡا لَوۡ تُدۡهِنُ فَيُدۡهِنُوۡنَ ﴿۱۰﴾

10. Wanapenda ungalikuwa laini (kwao), nao wakawa laini (kwako).

وَلَا تُطِعۡ كُلَّ حَلَّافٍ مَّهِيۡنٍ ۙ﴿۱۱﴾

11. Wala usimtii kila mwapaji sana, aliye dhalili,

هَمَّازٍ مَّشَّآءٍۭ بِنَمِيۡمٍ ۙ﴿۱۲﴾

12. Msingiziaji, aendaye akisengenya,

مَّنَّاعٍ لِّلۡخَيۡرِ مُعۡتَدٍ اَثِيۡمٍ ۙ﴿۱۳﴾

13. Akatazaye heri, arukaye mipaka, mwenye hatia.

عُتُلٍّۭ بَعۡدَ ذٰلِكَ زَنِيۡمٍ ۙ﴿۱۴﴾

14. Mwovu, (na) juu ya hayo mwana haramu,

اَنۡ كَانَ ذَا مَالٍ وَّبَنِيۡنَ ؕ﴿۱۵﴾

15. Ingawa ni mwenye mali na watoto.

اِذَا تُتۡلٰى عَلَيۡهِ اٰيٰتُنَا قَالَ اَسَاطِيۡرُ الۡاَوَّلِيۡنَ ﴿۱۶﴾

16. Anaposomewa Aya Zetu husema: Ni visa vya watu wa zamani.

سَنَسِمُهٗ عَلَى الۡخُرۡطُوۡمِ ﴿۱۷﴾

17. Karibuni Tutamtia kovu juu ya pua.

اِنَّا بَلَوۡنٰهُمۡ كَمَا بَلَوۡنَاۤ اَصۡحٰبَ

18. Hakika Tumewajaribu kama Tulivyowajaribu wenye bustani,

Aya 7. *Ni nani mwenye kichaa.* Ushindi wa Makka walioshinda Waislamu na makafiri wakanyang'anywa mamlaka ya mji ule mtakatifu ulihakikisha ni nani katika wao na Mtume, aliyekuwa na maneno ya ukichaa. Maneno ya Mtume *s.a.w.* yangekuwa ya wehu bishara hizi zisingetimia na makafiri wasingeshindwa na kunyang'anywa mji wa Makka.

Aya 11. Inasemekana mtu aliyetajwa hapa alikuwa Walid bin Mughira (Jamii' al-Bayan) au Abu Jahl, au Aswad bin Abd Yaghuth, au Akhnas bin Sharik (Razi). Aya ya 9 inaonyesha kuwa hali hizi ni za wale waliomkadhibisha Mtume s.a.w.

Aya 17. Katika vita vya Badri pua ya Walid bin Mughira ilikatwa na akabaki na kovu mpaka kufa kwake, na ubashiri huu uliotabiriwa katika Aya hii ukatimia.

walipoapa kwamba watayakata (matunda yake) itakapokuwa asubuhi,

الْجَنَّةِ ۚ اِذْ اَقْسَمُوْا لَيَصْرِمُنَّهَا مُصْبِحِيْنَ ﴿١٨﴾

19. Wala hawakusema, Insha-Allah:

وَلَا يَسْتَثْنُوْنَ ﴿١٩﴾

20. Basi uliizingia (bustani) msiba mkubwa utokao kwa Mola wako na hali wao walikuwa wanalala.

فَطَافَ عَلَيْهَا طَآئِفٌ مِّنْ رَّبِّكَ وَهُمْ نَآئِمُوْنَ ﴿٢٠﴾

21. Kwa hiyo ikawa kama iliyong'olewa.

فَاَصْبَحَتْ كَالصَّرِيْمِ ﴿٢١﴾

22. Asubuhi wakaitana,

فَتَنَادَوْا مُصْبِحِيْنَ ﴿٢٢﴾

23. Ya kwamba nendeni mapema kondeni mwenu ikiwa mnataka kuvuna.

اَنِ اغْدُوْا عَلٰى حَرْثِكُمْ اِنْ كُنْتُمْ صٰرِمِيْنَ ﴿٢٣﴾

24. Basi walikwenda huku wakinong'onezana,

فَانْطَلَقُوْا وَهُمْ يَتَخَافَتُوْنَ ﴿٢٤﴾

25. Wakisema: Leo maskini asiingie humo mwenu asilan kinyume cha mafao yenu.

اَنْ لَّا يَدْخُلَنَّهَا الْيَوْمَ عَلَيْكُمْ مِّسْكِيْنٌ ﴿٢٥﴾

26. Na wakaenda asubuhi na mipango ya kutompa yeyote chochote.

وَّغَدَوْا عَلٰى حَرْدٍ قٰدِرِيْنَ ﴿٢٦﴾

27. Basi walipoliona wakasema: Kwa hakika tumepotea.

فَلَمَّا رَاَوْهَا قَالُوْٓا اِنَّا لَضَآلُّوْنَ ﴿٢٧﴾

28. Bali tumenyimwa.

بَلْ نَحْنُ مَحْرُوْمُوْنَ ﴿٢٨﴾

29. Mbora wao akasema: Je, sikuwaambieni mbona hamumtukuzi (Allah)?

قَالَ اَوْسَطُهُمْ اَلَمْ اَقُلْ لَّكُمْ لَوْلَا تُسَبِّحُوْنَ ﴿٢٩﴾

30. Wakasema: Utukufu ni wa Mola wetu, hakika tulikuwa wadhalimu.

قَالُوْا سُبْحٰنَ رَبِّنَآ اِنَّا كُنَّا ظٰلِمِيْنَ ﴿٣٠﴾

31. Basi wakakabiliana wao kwa wao wakilaumiana

فَاَقْبَلَ بَعْضُهُمْ عَلٰى بَعْضٍ يَّتَلَاوَمُوْنَ ﴿٣١﴾

32. Wakasema: Ole wetu! hakika tulikuwa wapitao kiasi:

قَالُوْا يٰوَيْلَنَآ اِنَّا كُنَّا طٰغِيْنَ ﴿٣٢﴾

33. Asaa Mola wetu Atatubadilishia (konde) lililo bora kuliko hili; hakika sisi tunageuka kwa Mola wetu.

عَسٰى رَبُّنَآ اَنْ يُّبْدِلَنَا خَيْرًا مِّنْهَآ اِنَّآ اِلٰى رَبِّنَا رٰغِبُوْنَ ﴿٣٣﴾

Aya 26. *'Alaa hardin,* "Kuzuia" Neno hili pia maana yake ni "ubahili," na pia maana yake ni "kwa upesi" (Baidhawi).

كَذٰلِكَ الْعَذَابُ ۖ وَلَعَذَابُ الْاٰخِرَةِ
اَكْبَرُ ۘ لَوْ كَانُوْا يَعْلَمُوْنَ ﴿٣٤﴾ ع

34. Adhabu huwa namna hii, na adhabu ya Akhera ni kubwa zaidi, laiti wangalijua!

FUNGU 2

اِنَّ لِلْمُتَّقِيْنَ عِنْدَ رَبِّهِمْ جَنّٰتِ
النَّعِيْمِ ﴿٣٥﴾

35. Hakika wamchao Allah watakuwa na Bustani zenye neema kwa Mola wao.

اَفَنَجْعَلُ الْمُسْلِمِيْنَ كَالْمُجْرِمِيْنَ ﴿٣٦﴾

36. Je, Tuwafanye wanaotii sawa na wakosefu?

مَا لَكُمْ ۪ كَيْفَ تَحْكُمُوْنَ ﴿٣٧﴾ ۚ

37. Mmekuwaje mnahukumu namna gani?

اَمْ لَكُمْ كِتٰبٌ فِيْهِ تَدْرُسُوْنَ ﴿٣٨﴾

38. Au mnacho kitabu mkisomacho:

اِنَّ لَكُمْ فِيْهِ لَمَا تَخَيَّرُوْنَ ﴿٣٩﴾ ۚ

39. Hakika yatakuwamo kwa ajili yenu mnayoyachagua?

اَمْ لَكُمْ اَيْمَانٌ عَلَيْنَا بَالِغَةٌ اِلٰى
يَوْمِ الْقِيٰمَةِ ۙ اِنَّ لَكُمْ لَمَا تَحْكُمُوْنَ ﴿٤٠﴾ ۚ

40. Au je, mnavyo viapo juu Yetu vinavyofika mpaka siku ya Kiyama ya kuwa ninyi budi mtapata mnayoyahukumu?

سَلْهُمْ اَيُّهُمْ بِذٰلِكَ زَعِيْمٌ ﴿٤١﴾ ۚ

41. Waulize: Ni nani miongoni mwao mdhamini wa hayo.

اَمْ لَهُمْ شُرَكَآءُ ۚ فَلْيَاْتُوْا بِشُرَكَآئِهِمْ
اِنْ كَانُوْا صٰدِقِيْنَ ﴿٤٢﴾

42. Au je, wana washirika? Basi wawalete washirika wao wakiwa wanasema kweli.

يَوْمَ يُكْشَفُ عَنْ سَاقٍ وَّيُدْعَوْنَ اِلَى
السُّجُوْدِ فَلَا يَسْتَطِيْعُوْنَ ﴿٤٣﴾ ۙ

43. Siku ambayo kutakuwa na mfadhaiko mkubwa, na wataitwa kusujudu lakini hawataweza,

خَاشِعَةً اَبْصَارُهُمْ تَرْهَقُهُمْ ذِلَّةٌ ۭ
وَقَدْ كَانُوْا يُدْعَوْنَ اِلَى السُّجُوْدِ
وَهُمْ سٰلِمُوْنَ ﴿٤٤﴾

44. Macho yao yakiinama, fedheha itawafunika; na hakika walikuwa wakiitwa kusujudu walipokuwa salama.

فَذَرْنِيْ وَمَنْ يُّكَذِّبُ بِهٰذَا الْحَدِيْثِ ۭ
سَنَسْتَدْرِجُهُمْ مِّنْ حَيْثُ لَا يَعْلَمُوْنَ ﴿٤٥﴾ ۙ

45. Basi uniache na anayeikadhibisha hadithi hii; karibuni Tutawavuta kidogo kidogo kwa mahali wasipopajua.

Aya 43. *Yukshafu 'an saaqin,* "mateso makali" ndio hasa mradi wa maneno haya ya *muhawara (fumbo).* Pia maana yake ni siku "itakapodhihirika hakika." Na maana ya neno kwa neno ya *yukshafu 'an saaqin* ni siku "nguo itakapopandishwa miundini."

وَ اُمۡلِیۡ لَهُمۡ ؕ اِنَّ كَیۡدِیۡ مَتِیۡنٌ ﴿۴۶﴾

46. Na Ninawapa muhula, kwa hakika mpango wangu ni madhubuti.

اَمۡ تَسۡـَٔلُهُمۡ اَجۡرًا فَهُمۡ مِّنۡ مَّغۡرَمٍ مُّثۡقَلُوۡنَ ﴿۴۷﴾

47. Au je, unawaomba ujira nao wamelemewa na deni?

اَمۡ عِنۡدَهُمُ الۡغَیۡبُ فَهُمۡ یَكۡتُبُوۡنَ ﴿۴۸﴾

48. Au iko kwao (elimu ya) siri nao wanaiandika?

فَاصۡبِرۡ لِحُكۡمِ رَبِّكَ وَلَا تَكُنۡ كَصَاحِبِ الۡحُوۡتِ ۘ اِذۡ نَادٰی وَهُوَ مَكۡظُوۡمٌ ﴿۴۹﴾ ۘ

49. Basi subiri hukumu ya Mola wako, wala usiwe kama sahibu wa nyangumi, alipomwita (Allah) na hali yeye alikuwa mwenye huzuni nyingi.

لَوۡلَاۤ اَنۡ تَدٰرَكَهٗ نِعۡمَةٌ مِّنۡ رَّبِّهٖ لَنُبِذَ بِالۡعَرَآءِ وَهُوَ مَذۡمُوۡمٌ ﴿۵۰﴾

50. Kama isingalimfikia neema kutoka kwa Mola wake, bila shaka angalitupwa ufukoni na hali yu mwenye kulaumiwa.

فَاجۡتَبٰهُ رَبُّهٗ فَجَعَلَهٗ مِنَ الصّٰلِحِیۡنَ ﴿۵۱﴾

51. Lakini Mola wake Alimchagua na Akamfanya miongoni mwa watu wema.

وَ اِنۡ یَّكَادُ الَّذِیۡنَ كَفَرُوۡا لَیُزۡلِقُوۡنَكَ بِاَبۡصَارِهِمۡ لَمَّا سَمِعُوا الذِّكۡرَ وَ یَقُوۡلُوۡنَ اِنَّهٗ لَمَجۡنُوۡنٌ ۘ ﴿۵۲﴾

52. Na karibu wale wanaokufuru wangekutelezesha kwa (ukodozi wa) macho yao wanapoyasikia mawaidha, na husema: Hakika yeye ni majnuni.

وَمَا هُوَ اِلَّا ذِكۡرٌ لِّلۡعٰلَمِیۡنَ ﴿۵۲﴾

53. Na hiyo siyo ila ni nasaha kwa walimwengu.

Aya 49. *Sahibu wa nyangumi* ni Nabii Yunus, soma sura 37:43.

Aya 53. *Dhikr*. Neno hili tumelifasiri "ukumbusho" na pia maana yake ni heshima na ukubwa, yaani watakaofuata mafundisho ya Qur'an watapata heshima na utukufu. Na kweli, Waislamu waliofuata mafundisho haya walipata heshima kubwa duniani. Je, mafundisho ya majnuni gani yanayoweza kuleta matokeo ya namna hii?

سُوْرَةُ الْحَآقَّةِ مَكِّيَّةٌ وَّ هِيَ مَعَ الْبَسْمَلَةِ ثَلَاثٌ وَّ خَمْسُوْنَ اٰيَةً وَّ رُكُوْعَانِ

69. SURA AL-HAAQQA

Imeteremshwa Makka

Ina mafungu 2 na Aya 53 pamoja na Bismillahi

بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ ①

1. Kwa jina la Allah, Mwingi wa rehema, Mwingi wa ukarimu.

اَلْحَآقَّةُ ۙ② 2. Tukio la haki!

مَا الْحَآقَّةُ ۚ③ 3. Tukio la haki ni nini?

وَمَآ اَدْرٰىكَ مَا الْحَآقَّةُ ؕ④ 4. Na nini kitakujulisha tukio la haki ni nini?

كَذَّبَتْ ثَمُوْدُ وَعَادٌۢ بِالْقَارِعَةِ ⑤ 5. Wathamudi na Waadi walilikadhibisha balaa lenye kuangamiza.

فَاَمَّا ثَمُوْدُ فَاُهْلِكُوْا بِالطَّاغِيَةِ ⑥ 6. Basi Wathamudi waliangamizwa kwa balaa kubwa.

وَاَمَّا عَادٌ فَاُهْلِكُوْا بِرِيْحٍ صَرْصَرٍ عَاتِيَةٍ ۙ⑦ 7. Na ama Waadi waliangamizwa kwa upepo mkali usiozuilika,

سَخَّرَهَا عَلَيْهِمْ سَبْعَ لَيَالٍ وَّ ثَمٰنِيَةَ اَيَّامٍ ۙ حُسُوْمًا ۙ فَتَرَى الْقَوْمَ فِيْهَا صَرْعٰى ۙ كَاَنَّهُمْ اَعْجَازُ نَخْلٍ خَاوِيَةٍ ۚ⑧ 8. Aliowapelekea kwa mausiku saba na michana minane mfululizo, utaona watu wameanguka kifudifudi kana kwamba ni magogo ya mitende yenye uvungu.

Sura hii imepata jina katika Aya yake ya 2 inayowapa habari makafiri ya *msiba* utakaowafikia, na wanahakikishiwa jambo hili kwa kukumbushwa ajali zilizowafikia watu wa zamani waliokadhibisha Mitume. Sura hii ilishuka Makka.

Aya 2. *Al-Haaqqah,* "tukio la haki." Neno *Al-Haaqqah* maana yake ni "Haki" au "Kweli." na linafasiriwa kwa namna nyingi: (1) msiba mzito ambao kutokea kwake ni lazima (Kamus, Lane); (2) saa itakayokuja tokea au saa itakayokuwa na msiba mzito (Razi); (3) au saa ambayo mambo yatajulikana kabisa (Lane); au (4) saa ambayo matendo yatalipwa (Razi).

Tukio hili lililotajwa hapa ambalo litahakikisha kushinda kwa waaminio na kushindwa kwa makafiri limewekewa wakati ambao bila shaka litatokea.

Aya 5. Kwa kweli hii imechukuliwa toka katika maelezo ya Qur'an yenyewe ambamo *al-qaariah* imeelezwa kuwa ni *yauma yakuunu-naasu kalfaraashil mabthuuthi wa takuunul jibaalu kal'ihnil mamfuushi* (Suratl Qaariah aya ya 5-6) (101:5-6). Siku ambapo wanadamu watakuwa kama nondo waliotawanywa, na milima itakuwa kama hariri iliyochambuliwa.

Kwa hiyo siyo angamizo dogo bali inalirejea balaa kubwa sana kama lile linaloletwa na bomu la Haidrojeni na bomu la Nyutroni na kadhalika. Ukubwa wa mlipuko uliotajwa ni wa kiasi cha kuweza kuifanya milima kuwa vumbi.

فَهَلْ تَرٰى لَهُمْ مِّنْۢ بَاقِيَةٍ ۝٨

9. Basi je! utamwona mmoja wao aliyebaki?

وَجَآءَ فِرْعَوْنُ وَمَنْ قَبْلَهٗ وَالْمُؤْتَفِكٰتُ بِالْخَاطِئَةِ ۝٩

10. Na Firauni na waliomtangulia na (watu wa) miji iliyopinduliwa walikosa,

فَعَصَوْا رَسُوْلَ رَبِّهِمْ فَاَخَذَهُمْ اَخْذَةً رَّابِيَةً ۝١٠

11. Na wakamwasi Mtume wa Mola wao ndipo Akawakamata kwa mkamato wenye nguvu sana.

اِنَّا لَمَّا طَغَا الْمَآءُ حَمَلْنٰكُمْ فِى الْجَارِيَةِ ۝١١

12. Maji yalipofurika hakika Sisi Tuliwapandisheni katika merikebu,

لِنَجْعَلَهَا لَكُمْ تَذْكِرَةً وَّتَعِيَهَآ اُذُنٌ وَّاعِيَةٌ ۝١٢

13. Ili Tuifanye ukumbusho kwenu na sikio lisikialo liushike.

فَاِذَا نُفِخَ فِى الصُّوْرِ نَفْخَةٌ وَّاحِدَةٌ ۝١٣

14. Na litakapopulizwa baragumu mpulizo mmoja,

وَّحُمِلَتِ الْاَرْضُ وَالْجِبَالُ فَدُكَّتَا دَكَّةً وَّاحِدَةً ۝١٤

15. Na ardhi na milima vitaondolewa na vitavunjwa mvunjiko mmoja,

فَيَوْمَئِذٍ وَّقَعَتِ الْوَاقِعَةُ ۝١٥

16. Basi siku hiyo tukio litatokea.

وَانْشَقَّتِ السَّمَآءُ فَهِىَ يَوْمَئِذٍ وَّاهِيَةٌ ۝١٦

17. Na mbingu itapasuka, nayo siku hiyo, itakuwa dhaifu.

وَّالْمَلَكُ عَلٰٓى اَرْجَآئِهَا ؕ وَيَحْمِلُ عَرْشَ رَبِّكَ فَوْقَهُمْ يَوْمَئِذٍ ثَمٰنِيَةٌ ۝١٧

18. Na Malaika watakuwa wamesimama kandoni mwake, na siku hiyo juu yao Malaika wanane watakibeba kiti cha Enzi cha Mola wako.

يَوْمَئِذٍ تُعْرَضُوْنَ لَا تَخْفٰى مِنْكُمْ خَافِيَةٌ ۝١٨

19. Siku hiyo mtahudhurishwa- haitafichika kwenu siri yo yote.

فَاَمَّا مَنْ اُوْتِىَ كِتٰبَهٗ بِيَمِيْنِهٖ ۙ فَيَقُوْلُ هَآؤُمُ اقْرَءُوْا كِتٰبِيَهْ ۝١٩

20. Basi ama yule atakayepewa daftari yake kwa mkono wake wa kuume, atasema: Haya! Someni daftari yangu:

اِنِّىْ ظَنَنْتُ اَنِّىْ مُلٰقٍ حِسَابِيَهْ ۝٢٠

21. Hakika nilijua ya kuwa nita pokea hesabu yangu.

فَهُوَ فِىْ عِيْشَةٍ رَّاضِيَةٍ ۝٢١

22. Basi yeye atakuwa katika maisha ya raha.

فِىْ جَنَّةٍ عَالِيَةٍ ۝٢٢

23. Katika Bustani iliyo juu,

قُطُوْفُهَا دَانِيَةٌ ۝٢٣

24. Vishada vyake vitakuwa karibu:

كُلُوْا وَاشْرَبُوْا هَنِيْٓـًٔا بِمَآ اَسْلَفْتُمْ فِى الْاَيَّامِ الْخَالِيَةِ ۝٢٤

25. Kuleni na kunyweni kwa furaha kwa sababu ya vitendo mlivyofanya katika siku zilizopita.

وَاَمَّا مَنْ اُوْتِيَ كِتٰبَهٗ بِشِمَالِهٖ ۙ
فَيَقُوْلُ يٰلَيْتَنِيْ لَمْ اُوْتَ كِتٰبِيَهْ ۚ﴿٢٦﴾

26. Walakini atakayepewa daftari yake katika mkono wake wa kushoto, basi yeye atasema: Oo! Laiti nisingalipewa daftari yangu:

وَلَمْ اَدْرِ مَا حِسَابِيَهْ ۚ﴿٢٧﴾

27. Wala nisingalijua ni nini hesabu yangu:

يٰلَيْتَهَا كَانَتِ الْقَاضِيَةَ ۚ﴿٢٨﴾

28. Laiti mauti yangenimaliza kabisa.

مَآ اَغْنٰى عَنِّيْ مَالِيَهْ ۚ﴿٢٩﴾

29. Mali yangu haikunifaa.

هَلَكَ عَنِّيْ سُلْطٰنِيَهْ ۚ﴿٣٠﴾

30. Usultani wangu umenipotea.

خُذُوْهُ فَغُلُّوْهُ ۙ﴿٣١﴾

31. Mkamateni na mtieni minyororo shingoni mwake,

ثُمَّ الْجَحِيْمَ صَلُّوْهُ ۙ﴿٣٢﴾

32. Kisha mtupeni Motoni,

ثُمَّ فِيْ سِلْسِلَةٍ ذَرْعُهَا سَبْعُوْنَ ذِرَاعًا
فَاسْلُكُوْهُ ؕ﴿٣٣﴾

33. Tena katika mnyororo wenye urefu wa dhiraa sabini mwingizeni.

اِنَّهٗ كَانَ لَا يُؤْمِنُ بِاللّٰهِ الْعَظِيْمِ ۙ﴿٣٤﴾

34. Hakika yeye alikuwa hamwamini Allah, Adhimu.

وَلَا يَحُضُّ عَلٰى طَعَامِ الْمِسْكِيْنِ ؕ﴿٣٥﴾

35. Wala hakuhimiza juu ya kulisha maskini.

فَلَيْسَ لَهُ الْيَوْمَ هٰهُنَا حَمِيْمٌ ۙ﴿٣٦﴾

36. Basi leo hapa hana rafiki mpenzi'

وَّلَا طَعَامٌ اِلَّا مِنْ غِسْلِيْنٍ ۙ﴿٣٧﴾

37. Wala chakula cho chote ila maji yaliyooshewa vidonda.

لَّا يَاْكُلُهٗۤ اِلَّا الْخَاطِـُٔوْنَ ۚ﴿٣٨﴾ ع ١

38. (Na) hawali (chakula) hicho ila wakosefu tu.

FUNGU 2

فَلَاۤ اُقْسِمُ بِمَا تُبْصِرُوْنَ ۙ﴿٣٩﴾

39. Basi naapa kwa mnavyoviona,

وَمَا لَا تُبْصِرُوْنَ ۙ﴿٤٠﴾

40. Na msivyoviona.

اِنَّهٗ لَقَوْلُ رَسُوْلٍ كَرِيْمٍ ۚ﴿٤١﴾

41. Kwa hakika hii ni kauli ya Mtume mwenye heshima.

وَّمَا هُوَ بِقَوْلِ شَاعِرٍ ؕ قَلِيْلًا مَّا
تُؤْمِنُوْنَ ۙ﴿٤٢﴾

42. Wala hiyo si kauli ya mshairi; ni kidogo tu mnayoyaamini.

وَلَا بِقَوْلِ كَاهِنٍ ؕ قَلِيْلًا مَّا تَذَكَّرُوْنَ ؕ﴿٤٣﴾

43. Wala hiyo si kauli ya kahini; ni nasaha ndogo tu mnayoikamata.

تَنْزِيْلٌ مِّنْ رَّبِّ الْعٰلَمِيْنَ ﴿٤٤﴾

44. Ni uteremsho kutoka kwa Mola wa walimwengu wote.

وَلَوْ تَقَوَّلَ عَلَيْنَا بَعْضَ الْاَقَاوِيْلِ ﴿٤٥﴾

45. Na kama (Mtume) angelizua juu yetu baadhi ya maneno,

لَاَخَذْنَا مِنْهُ بِالْيَمِيْنِ ﴿٤٦﴾

46. Bila shaka Tungalimshika kwa mkono wa kuume,

ثُمَّ لَقَطَعْنَا مِنْهُ الْوَتِيْنَ ﴿٤٧﴾

47. Kisha kwa hakika Tungali mkata mshipa mkubwa (wa moyo).

فَمَا مِنْكُمْ مِّنْ اَحَدٍ عَنْهُ حٰجِزِيْنَ ﴿٤٨﴾

48. Na hakuna ye yote katika ninyi ambaye angeweza kumkinga Tusimfikie.

وَ اِنَّهٗ لَتَذْكِرَةٌ لِّلْمُتَّقِيْنَ ﴿٤٩﴾

49. Kwa hakika hii ni nasaha kubwa kwa wamchao Mungu.

وَ اِنَّا لَنَعْلَمُ اَنَّ مِنْكُمْ مُّكَذِّبِيْنَ ﴿٥٠﴾

50. Na kwa yakini Tunajua ya kuwa miongoni mwenu wamo wanaokadhibisha.

وَ اِنَّهٗ لَحَسْرَةٌ عَلَى الْكٰفِرِيْنَ ﴿٥١﴾

51. Na kwa kweli hilo ni sikitiko juu ya wanaokataa.

وَ اِنَّهٗ لَحَقُّ الْيَقِيْنِ ﴿٥٢﴾

52. Na kwa hakika hiyo ni haki ya yakini.

فَسَبِّحْ بِاسْمِ رَبِّكَ الْعَظِيْمِ ﴿٥٣﴾ ع

53. Basi litukuze jina la Mola wako Aliye Mkuu.

Aya 46. *Tungalimshika kwa mkono wa kuume.* Maana zake mbili: (1) Mkono wa kuume wa Mtume *s.a.w.* ungeshikwa, na nguvu zake zingenyang'anywa na angeuawa; (2) Mungu angemshika kwa Mkono wa Kuume, yaani angemshika barabbara na kumwadhibu kwa kifo.

Hiyo ndiyo kanuni iliyoelezwa katika chuo cha Nabii Musa (Kumbukumbu la Torati 18:20; 13:5) Mwenye kumzulia Mungu uwongo huangamizwa na upanga na njaa, (Jer. 14:15). Mvua kali ya hasira na ghadhabu ya Allah humkomesha (Ezekiel 13:13). Hiyo ni desturi ya Allah tangu awali mpaka sasa, ijulikanayo katika kila nchi na kila karne, kumwangamiza mwongo na kumnusuru mkweli. Mtume Muhammad *s.a.w.* angekuwa mtunga uwongo, jinsi wadhanivyo watu walalamishi, asingefaulu. Adui zake ndio walioteketezwa na upanga na njaa na adhabu nyingine kali. Kwa sababu kwa kumkadhibisha mwenye haki huyo walionekana kuwa wanapigana na Mungu (Matendo 5:34-39).

Ikumbukwe ya kuwa Aya hii imeeleza kanuni moja ya kuwa kama mtu atangaze ufunuo kuwa amepewa na Mungu na ametumwa naye, hali Mungu hakumtuma na aendelee na madai yake hayo ya uwongo, hawezi kuishi miaka 23 ila atauawa kabla ya umri huo. Na hii ndiyo dalili nyingine mojawapo inayopambanua madai ya Nabii wa kweli; kama mtu adai unabii na aweze kuishi miaka 23 au zaidi toka kudai kwake, yeye bila shaka atakuwa Mjumbe wa kweli. Soma *Sharha 'Aqaaid Nasafi* kitabu mashuhuri cha *'aqaaid za Ahli Sunnat wal Jamaa't,* ambacho kinasema, "Akili haikubali ya kuwa mambo haya yote yakusanyike katika watu wasiokuwa Manabii na hali Allah anajua kuwa anamtungia uwongo, kisha ampe muda wa miaka 23" (uk. 100). Imam Ibni Kayyim anasema katika kitabu chake *Zaad al-Maad* ya kuwa, "inawezekanaje mtu amtungie Allah uwongo na Mungu asimwangamize bali amsaidie? Mtu anayesaidiwa namna hii hawezi kuwa mwongo.

Kipimo hiki cha miaka 23 wametoa katika jambo hili: Mtume alidai utume alipokuwa na umri wa miaka 40 na akafariki alipokuwa na umri wa miaka 63, ikawa ameishi miaka 23 toka kudai utume wake. Basi mtu atakayepata muda wa miaka 23 baada ya kudai kuwa anapokea ufunuo, hawezi kuwa mwongo.

سُوْرَةُ الْمَعَارِجِ مَكِّيَّةٌ وَّ هِيَ مَعَ الْبَسْمَلَةِ خَمْسٌ وَّ اَرْبَعُوْنَ اٰيَةً وَّ رُكُوْعَانِ

70. SURA AL-MA'AARIJ

Imeteremshwa Makka

Ina mafungu 2 na Aya 45 pamoja na Bismillahi

بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ ①

1. Kwa jina la Allah, Mwingi wa rehema, Mwingi wa ukarimu.

سَاَلَ سَآئِلٌۢ بِعَذَابٍ وَّاقِعٍ ②

2. Mwulizaji aliuliza juu ya adhabu itakayotokea,

لِّلْكٰفِرِيْنَ لَيْسَ لَهٗ دَافِعٌ ③

3. Juu ya makafiri - hapana awezaye kuizuia.

مِّنَ اللّٰهِ ذِى الْمَعَارِجِ ④

4. Kutoka kwa Allah, Mwenye madaraja ya juu.

تَعْرُجُ الْمَلٰٓئِكَةُ وَالرُّوْحُ اِلَيْهِ فِىْ يَوْمٍ كَانَ مِقْدَارُهٗ خَمْسِيْنَ اَلْفَ سَنَةٍ ۚ ⑤

5. Malaika na Roho hupanda Kwake katika siku iliyo muda wake miaka elfu hamsini.

فَاصْبِرْ صَبْرًا جَمِيْلًا ⑥

6. Basi subiri kwa subira njema.

اِنَّهُمْ يَرَوْنَهٗ بَعِيْدًا ⑦

7. Kwa hakika wao wanaiona i mbali,

وَّنَرٰىهُ قَرِيْبًا ⑧

8. Nasi Tunaiona i karibu.

يَوْمَ تَكُوْنُ السَّمَآءُ كَالْمُهْلِ ⑨

9. Siku mbingu itakapokuwa kama shaba iliyoyeyuka,

وَتَكُوْنُ الْجِبَالُ كَالْعِهْنِ ⑩

10. Na milima itakuwa kama sufi,

وَلَا يَسْـَٔلُ حَمِيْمٌ حَمِيْمًا ⑪

11. Wala rafiki hatamwuliza rafiki (yake),

يُّبَصَّرُوْنَهُمْ يَوَدُّ الْمُجْرِمُ لَوْ يَفْتَدِىْ مِنْ عَذَابِ يَوْمِئِذٍۭ بِبَنِيْهِ ⑫

12. Watafanywa waonane; mwenye kosa atapenda walau ajikomboe katika adhabu ya Siku hiyo kwa kulipa watoto wake,

وَصَاحِبَتِهٖ وَاَخِيْهِ ⑬

13. Na mke wake na ndugu yake,

وَفَصِيْلَتِهِ الَّتِىْ تُـْٔوِيْهِ ⑭

14. Na jamaa zake waliokuwa wa-kimhifadhi,

Jina la sura hii linatokea katika Aya 2. Sura hii ilishuka Makka.

Aya 5. *Siku iliyo muda wake miaka elfu hamsini.* Hapa inaonekana ya kuwa siku za Allah ni tofauti na siku zetu za saa 24. Hapa tunaambiwa pengine siku moja ya Allah inaweza kuwa sawa na miaka yetu hamsini elfu (50,000).

وَمَنْ فِي الْاَرْضِ جَمِيْعًا ۙ ثُمَّ يُنْجِيْهِ ﴿١٥﴾

15. Na (kulipa) vyote vilivyomo ardhini, kisha vimuokoe.

كَلَّا ؕ اِنَّهَا لَظٰى ﴿١٦﴾

16. Sivyo! Kwa hakika huo ni Moto uwakao,

نَزَّاعَةً لِّلشَّوٰى ﴿١٧﴾

17. Uchubuao ngozi ya mwili.

تَدْعُوْا مَنْ اَدْبَرَ وَتَوَلّٰى ﴿١٨﴾

18. Utamwita kila aliyegeuza mgongo na akageuka,

وَجَمَعَ فَاَوْعٰى ﴿١٩﴾

19. Na akakusanya, kisha akahifadhi.

اِنَّ الْاِنْسَانَ خُلِقَ هَلُوْعًا ﴿٢٠﴾

20. Kwa hakika mtu aliumbwa hali ya kuwa mwenye pupa.

اِذَا مَسَّهُ الشَّرُّ جَزُوْعًا ﴿٢١﴾

21. Inapomshika shari huwa mwenye fadhaa.

وَّاِذَا مَسَّهُ الْخَيْرُ مَنُوْعًا ﴿٢٢﴾

22. Na inapomshika heri huwa bahili;

اِلَّا الْمُصَلِّيْنَ ﴿٢٣﴾

23. Ila wanaosali,

الَّذِيْنَ هُمْ عَلٰى صَلَاتِهِمْ دَآئِمُوْنَ ﴿٢٤﴾

24. Ambao wanadumu katika Sala zao,

وَالَّذِيْنَ فِيْٓ اَمْوَالِهِمْ حَقٌّ مَّعْلُوْمٌ ﴿٢٥﴾

25. Na ambao katika mali zao iko haki maalumu,

لِّلسَّآئِلِ وَالْمَحْرُوْمِ ﴿٢٦﴾

26. Kwa ajili ya aombaye na maskini asiyeomba.

وَالَّذِيْنَ يُصَدِّقُوْنَ بِيَوْمِ الدِّيْنِ ﴿٢٧﴾

27. Na ambao wanaisadiki siku ya Malipo,

وَالَّذِيْنَ هُمْ مِّنْ عَذَابِ رَبِّهِمْ مُّشْفِقُوْنَ ﴿٢٨﴾

28. Na ni waiogopao adhabu (itokayo) kwa Mola wao.

اِنَّ عَذَابَ رَبِّهِمْ غَيْرُ مَاْمُوْنٍ ﴿٢٩﴾

29. Hakika adhabu ya Mola wao si ya kusalimika nayo

وَالَّذِيْنَ هُمْ لِفُرُوْجِهِمْ حٰفِظُوْنَ ﴿٣٠﴾

30. Na ambao wanahifadhi tupu zao.

اِلَّا عَلٰٓى اَزْوَاجِهِمْ اَوْ مَا مَلَكَتْ اَيْمَانُهُمْ فَاِنَّهُمْ غَيْرُ مَلُوْمِيْنَ ﴿٣١﴾

31. Isipokuwa kwa wake zao au wale iliyowamiliki mikono yao ya kuume -basi hao hawalaumiwi.

فَمَنِ ابْتَغٰى وَرَآءَ ذٰلِكَ فَاُولٰٓئِكَ هُمُ الْعٰدُوْنَ ﴿٣٢﴾

32. Lakini anayetaka kinyume cha hayo, basi hao ndio wanaoruka mipaka.

Aya 18-22. Katika Aya hizi zimeelezwa sifa za watu wa Motoni: (1) Kurudi nyuma katika haki; (2) kuipa haki kisogo; (3) kukusanya mali na kuificha; (4) kuwa na pupa; (5) akishikwa na shari anafadhaika na kukata tamaa; (6) akipata anakuwa bahili.

Aya 23. Toka Aya hii zimeelezwa sifa ambazo watakaozishika wataingia Peponi.

33. Na ambao wanaangalia amana zao na maagano yao.

وَالَّذِيْنَ هُمْ لِاَمٰنٰتِهِمْ وَعَهْدِهِمْ رٰعُوْنَ ﴿٣٢﴾

34. Na ambao ni imara katika ushahidi,

وَالَّذِيْنَ هُمْ بِشَهٰدٰتِهِمْ قَآئِمُوْنَ ﴿٣٣﴾

35. Na ambao wanazilinda Sala zao.

وَالَّذِيْنَ هُمْ عَلٰى صَلَاتِهِمْ يُحَافِظُوْنَ ﴿٣٤﴾

36. Hao ndio watakuwa katika Mabustani wakiheshimiwa.

اُولٰٓئِكَ فِيْ جَنّٰتٍ مُّكْرَمُوْنَ ﴿٣٥﴾ ع

FUNGU 2

37. Basi imekuwaje wanaokufuru wanakujia haraka,

فَمَالِ الَّذِيْنَ كَفَرُوْا قِبَلَكَ مُهْطِعِيْنَ ﴿٣٦﴾

38. Vikosi-vikosi kwa upande wa kulia na kwa upande wa kushoto?

عَنِ الْيَمِيْنِ وَعَنِ الشِّمَالِ عِزِيْنَ ﴿٣٧﴾

39. Je, kila mmoja wao anatumai kwamba ataingizwa katika bustani ya neema?

اَيَطْمَعُ كُلُّ امْرِئٍ مِّنْهُمْ اَنْ يُّدْخَلَ جَنَّةَ نَعِيْمٍ ﴿٣٨﴾

40. Sivyo! Hakika Tumewaumba katika kile wanachokijua.

كَلَّا ؕ اِنَّا خَلَقْنٰهُمْ مِّمَّا يَعْلَمُوْنَ ﴿٣٩﴾

41. Basi naapa kwa Mola wa mashariki zote na magharibi zote kwamba Sisi Tunaweza,

فَلَآ اُقْسِمُ بِرَبِّ الْمَشٰرِقِ وَالْمَغٰرِبِ اِنَّا لَقٰدِرُوْنَ ﴿٤٠﴾

42. Kuwabadili (na kuleta) walio wema kuliko wao, na Sisi sio wenye kushindwa.

عَلٰٓى اَنْ نُّبَدِّلَ خَيْرًا مِّنْهُمْ ۙ وَمَا نَحْنُ بِمَسْبُوْقِيْنَ ﴿٤١﴾

43. Basi waache wapige porojo na wacheze mpaka waione Siku yao wanayoahidiwa;

فَذَرْهُمْ يَخُوْضُوْا وَيَلْعَبُوْا حَتّٰى يُلٰقُوْا يَوْمَهُمُ الَّذِيْ يُوْعَدُوْنَ ﴿٤٢﴾

44. Siku watakapotoka makaburini kwa kasi kana kwamba wanakimbilia kwenye sehemu za machinjio

يَوْمَ يَخْرُجُوْنَ مِنَ الْاَجْدَاثِ سِرَاعًا كَاَنَّهُمْ اِلٰى نُصُبٍ يُّوْفِضُوْنَ ﴿٤٣﴾

45. Macho yao yatainama, fedheha itawafunikiza; hiyo ndiyo Siku waliyokuwa wakiahidiwa.

خَاشِعَةً اَبْصَارُهُمْ تَرْهَقُهُمْ ذِلَّةٌ ؕ ذٰلِكَ الْيَوْمُ الَّذِيْ كَانُوْا يُوْعَدُوْنَ ﴿٤٤﴾ ع

Aya 42. Angalieni jinsi bishara zinavyoelezwa wazi wazi ya kuwa nguvu ya makafiri itavunjwa na waaminio watatawala mahali pao.

Aya 44. *Makaburini.* Majumba ya makafiri yameitwa makaburi kwa kuwa kwa kiroho wao ni wafu. Na Aya 44 inaeleza hasa namna walivyokuwa makafiri siku mji wa Makka uliposhindwa na kutekwa na Waislamu.

سُوْرَةُ نُوْحٍ مَكِّيَّةٌ وَّ هِيَ مَعَ الْبَسْمَلَةِ تِسْعٌ وَّ عِشْرُوْنَ اٰيَةً وَّ رُكُوْعَانِ

71. SURA NUUH

Imeteremshwa Makka

Ina mafungu 2 na Aya 29 pamoja na Bismillahi

بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ ①

1. Kwa jina la Allah, Mwingi wa rehema, Mwingi wa ukarimu.

اِنَّاۤ اَرْسَلْنَا نُوْحًا اِلٰى قَوْمِهٖۤ اَنْ اَنْذِرْ قَوْمَكَ مِنْ قَبْلِ اَنْ يَّاْتِيَهُمْ عَذَابٌ اَلِيْمٌ ②

2. Hakika Sisi Tulimtuma Nuhu kwa watu wake, ya kwamba uwaonye watu wako kabla ya kuwafikia adhabu iumizayo.

قَالَ يٰقَوْمِ اِنِّيْ لَكُمْ نَذِيْرٌ مُّبِيْنٌ ۙ ③

3. Akasema: Enyi watu wangu! kwa hakika mimi ni Mwonyaji dhahiri kwenu,

اَنِ اعْبُدُوا اللّٰهَ وَاتَّقُوْهُ وَاَطِيْعُوْنِ ۙ ④

4. Ya kuwa Mwabuduni Allah na Mcheni na mnitii.

يَغْفِرْ لَكُمْ مِّنْ ذُنُوْبِكُمْ وَيُؤَخِّرْكُمْ اِلٰۤى اَجَلٍ مُّسَمًّى ؕ اِنَّ اَجَلَ اللّٰهِ اِذَا جَآءَ لَا يُؤَخَّرُ ۘ لَوْ كُنْتُمْ تَعْلَمُوْنَ ۝ ⑤

5. Atawasameheni madhambi yenu na Atawapeni muhula kwa muda fulani; hakika ifikapo ajali itokayo kwa Allah huwa haizuiliki: laiti mngejua!

قَالَ رَبِّ اِنِّيْ دَعَوْتُ قَوْمِيْ لَيْلًا وَّنَهَارًا ۙ ⑥

6. Akasema: Ee Mola wangu, kwa hakika niliwaita watu wangu usiku na mchana,

فَلَمْ يَزِدْهُمْ دُعَآءِيْۤ اِلَّا فِرَارًا ⑦

7. Lakini mwito wangu haukuwazidishia ila kukimbia.

وَاِنِّيْ كُلَّمَا دَعَوْتُهُمْ لِتَغْفِرَ لَهُمْ جَعَلُوْۤا

8. Na kila mara nilipowaita Uwasamehe, waliziba masikio yao kwa

---

Sura hii yote inaeleza habari za kazi ya Nabii Nuhu ya kubashiri dini, na maombi yake aliyowaombea wadhalimu kuangamizwa, ili uovu usistawi duniani. Sura hii ilishuka Makka.

Aya 4. Katika Aya hii yameelezwa mambo matatu ambayo kwa kuyashika mtu anaweza kuiepuka adhabu ya Allah: (1) kumwabudu Mungu; (2) kumwogopa na (3) kumtii Nabii.

Aya 8. Ndiyo desturi ya tangu zamani, kama Manabii wanafika watu wanakataa kusikiliza maneno yao na wanawakataza watu wengine pia wasisikilize. Kufanya hivi pia ni kiburi.

vidole vyao, na walijifunika nguo zao na wakadumu katika uovu wao, na wakafanya kiburi kingi.

اَصَابِعَهُمْ فِيْٓ اٰذَانِهِمْ وَاسْتَغْشَوْا ثِيَابَهُمْ وَاَصَرُّوْا وَاسْتَكْبَرُوا اسْتِكْبَارًا ۚ﴿٧﴾

9. Tena niliwaita kwa sauti kuu:

ثُمَّ اِنِّيْ دَعَوْتُهُمْ جِهَارًا ۙ﴿٩﴾

10. Kisha nikawatangazia na nikasema nao kwa siri:

ثُمَّ اِنِّيْٓ اَعْلَنْتُ لَهُمْ وَاَسْرَرْتُ لَهُمْ اِسْرَارًا ۙ﴿١٠﴾

11. Nikiwaambia: Ombeni msamaha kwa Mola wenu, hakika Yeye ni Msamehevu mno:

فَقُلْتُ اسْتَغْفِرُوْا رَبَّكُمْ ؕ اِنَّهٗ كَانَ غَفَّارًا ۙ﴿١١﴾

12. Atawaleteeni mawingu yanyeshayo mvua nyingi:

يُّرْسِلِ السَّمَآءَ عَلَيْكُمْ مِّدْرَارًا ۙ﴿١٢﴾

13. Na Atawasaidieni kwa mali na watoto, na Atawatengenezeeni mabustani, na Atawafanyieni mito.

وَّيُمْدِدْكُمْ بِاَمْوَالٍ وَّبَنِيْنَ وَيَجْعَلْ لَّكُمْ جَنّٰتٍ وَّيَجْعَلْ لَّكُمْ اَنْهٰرًا ؕ﴿١٣﴾

14. Mmekuwaje hamtarajii heshima kwa Allah?

مَا لَكُمْ لَا تَرْجُوْنَ لِلّٰهِ وَقَارًا ۚ﴿١٤﴾

15. Na hali Yeye Amewaumbeni kwa namna mbali mbali.

وَقَدْ خَلَقَكُمْ اَطْوَارًا ﴿١٥﴾

16. Je, hamwoni jinsi Allah Alivyoziumba mbingu saba tabaka-tabaka.

اَلَمْ تَرَوْا كَيْفَ خَلَقَ اللّٰهُ سَبْعَ سَمٰوٰتٍ طِبَاقًا ۙ﴿١٦﴾

17. Na Akaufanya mwezi ndani yake uwe nuru na Akalifanya jua kuwa taa?

وَّ جَعَلَ الْقَمَرَ فِيْهِنَّ نُوْرًا وَّ جَعَلَ الشَّمْسَ سِرَاجًا ﴿١٧﴾

18. Na Allah Akawaotesheni katika ardhi kama mimea:

وَ اللّٰهُ اَنْۢبَتَكُمْ مِّنَ الْاَرْضِ نَبَاتًا ۙ﴿١٨﴾

19. Kisha Atawarudisheni humo na Atawatoeni tena kwa namna mpya.

ثُمَّ يُعِيْدُكُمْ فِيْهَا وَيُخْرِجُكُمْ اِخْرَاجًا ﴿١٩﴾

20. Na Allah Aliwafanyieni ardhi kuwa tandiko,

وَاللّٰهُ جَعَلَ لَكُمُ الْاَرْضَ بِسَاطًا ۙ﴿٢٠﴾

21. Ili mtembee humo katika njia zilizo pana.

لِّتَسْلُكُوْا مِنْهَا سُبُلًا فِجَاجًا ۚ﴿٢١﴾

Aya 9-10. Hivi ndivyo wafanyavyo Manabii, wanatumia kila njia kuwafikishia watu ujumbe wa Allah ili wasalimike na wasiangamie.

FUNGU 2

قَالَ نُوْحٌ رَّبِّ اِنَّهُمْ عَصَوْنِيْ وَاتَّبَعُوْا مَنْ لَّمْ يَزِدْهُ مَالُهٗ وَوَلَدُهٗٓ اِلَّا خَسَارًا ﴿٢١﴾

22. Nuhu akasema: Mola wangu, hakika hao wameniasi na wakamfuata ambaye mali yake na watoto wake havikumzidishia ila hasara.

وَمَكَرُوْا مَكْرًا كُبَّارًا ﴿٢٢﴾

23. Na wakafanya hila kubwa.

وَقَالُوْا لَا تَذَرُنَّ اٰلِهَتَكُمْ وَلَا تَذَرُنَّ وَدًّا وَّلَا سُوَاعًا ۙ وَّلَا يَغُوْثَ وَيَعُوْقَ وَنَسْرًا ﴿٢٣﴾

24. Na wakasema: Msiache miungu yenu, wala msimwache Waddi, wala Suwa'an wala Yaghuthi na Yauki na Nasri.

وَقَدْ اَضَلُّوْا كَثِيْرًا ۚ وَلَا تَزِدِ الظّٰلِمِيْنَ اِلَّا ضَلٰلًا ﴿٢٤﴾

25. Nao wamekwisha wapoteza (watu) wengi wala Usiwazidishie wadhalimu ila kupotelea mbali!

مِمَّا خَطِيْٓـٰٔتِهِمْ اُغْرِقُوْا فَاُدْخِلُوْا نَارًا ۙ فَلَمْ يَجِدُوْا لَهُمْ مِّنْ دُوْنِ اللّٰهِ اَنْصَارًا ﴿٢٥﴾

26. Kwa ajili ya makosa yao waligharikishwa wakaingizwa Motoni; wala hawakuwapata wasaidizi kinyume cha Allah.

وَقَالَ نُوْحٌ رَّبِّ لَا تَذَرْ عَلَى الْاَرْضِ مِنَ الْكٰفِرِيْنَ دَيَّارًا ﴿٢٦﴾

27. Na Nuhu akasema: Mola wangu! Usiache juu ya ardhi mkazi ye yote katika makafiri.

اِنَّكَ اِنْ تَذَرْهُمْ يُضِلُّوْا عِبَادَكَ وَلَا يَلِدُوْٓا اِلَّا فَاجِرًا كَفَّارًا ﴿٢٧﴾

28. Hakika Ukiwaacha watawapoteza waja Wako wala hawatazaa ila (watoto) waovu wenye utovu mkubwa wa shukrani.

رَبِّ اغْفِرْ لِيْ وَلِوَالِدَيَّ وَلِمَنْ دَخَلَ بَيْتِيَ مُؤْمِنًا وَّلِلْمُؤْمِنِيْنَ وَالْمُؤْمِنٰتِ ۭ وَلَا تَزِدِ الظّٰلِمِيْنَ اِلَّا تَبَارًا ﴿٢٨﴾ ع

29. Mola wangu! Unighofirie mimi na wazee wangu, na kila aliyeingia nyumbani mwangu katika hali ya kuamini, na waaminio wanaume na waaminio wanawake; wala Usiwazidishie wadhalimu ila maangamizo!

Aya 27. Hii inaonyesha ya kuwa Manabii wanaweza kuwaombea watu wabaya waangamizwe. Na watu wanatakiwa waogope kabisa maana maombi ya namna hii ya Manabii huwa hayaendi bure, ila lazima yatawaletea watu adhabu, wasipotii. Pia katika adhabu za namna hii huwa rehema kwa ajili ya watu wengine ambao zinawasaidia kuwazidishia imani na kuwatia hofu wasifuate mwendo mbaya wa watu wanaowakataa Manabii.

سُوْرَةُ الْجِنِّ مَكِّيَّةٌ وَّ هِيَ مَعَ الْبَسْمَلَةِ تِسْعٌ وَّ عِشْرُوْنَ اٰيَةً وَّ رُكُوْعَانِ

72. SURA AL-JINN

Imeteremshwa Makka

Ina mafungu 2 na Aya 29 pamoja na Bismillahi

بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ ①

1. Kwa jina la Allah, Mwingi wa rehema, Mwingi wa ukarimu.

قُلْ اُوْحِيَ اِلَيَّ اَنَّهُ اسْتَمَعَ نَفَرٌ مِّنَ الْجِنِّ فَقَالُوْٓا اِنَّا سَمِعْنَا قُرْاٰنًا عَجَبًا ②

2. Sema: Imefunuliwa kwangu ya kuwa kundi la majinni walisikia wakasema: Hakika Tumeisikia Qur'an ya ajabu,

يَّهْدِيْٓ اِلَى الرُّشْدِ فَاٰمَنَّا بِهٖ ؕ وَلَنْ نُّشْرِكَ بِرَبِّنَآ اَحَدًا ③

3. Inaongoza kwenye uongofu, kwa hiyo tumeiamini, wala hatutamshirikisha ye yote na Mola wetu:

وَّاَنَّهٗ تَعٰلٰى جَدُّ رَبِّنَا مَا اتَّخَذَ صَاحِبَةً وَّلَا وَلَدًا ④

4. Na kwa hakika shani ya Mola wetu iko juu, Hakuchukua mke wala mwana:

وَّاَنَّهٗ كَانَ يَقُوْلُ سَفِيْهُنَا عَلَى اللّٰهِ شَطَطًا ⑤

5. Na kwa hakika mpumbavu miongoni mwetu alikuwa akisema maneno ya upuuzi juu ya Allah;

وَّاَنَّا ظَنَنَّآ اَنْ لَّنْ تَقُوْلَ الْاِنْسُ وَالْجِنُّ عَلَى اللّٰهِ كَذِبًا ⑥

6. Nasi tulikuwa tukidhani ya kuwa watu na majinni hawatasema uwongo juu ya Allah.

Sura hii inaeleza ulinzi wanaopata Manabii kwa Allah juu ya maadui zao. Jina la sura hii linatoka katika Aya ya 2 inayoeleza watu walioitwa *Jinn* waliomwamini Mtume *s.a.w.* Sura hii ilishuka Makka, wakati Mtume *s.a.w.* alipokuwa anarudi Makka kutoka Taif, miaka miwili kabla ya Hijra.

Aya 2. *Kundi moja la majinni.* Ingawa tunakiri kama vile Malaika ni viumbe pia kuna viumbe wanaoitwa majinni, lakini hatukiri kuwa kuna majinni wanaowakamata wanawake na watoto. Katika Hadithi neno *Jinn* limetumiwa kwa ajili ya vitu vingi kama mbwa mwehu, nyoka, nzi na vidudu vingine visivyoonekana kwa macho matupu. Kadhalika watu wakubwa wameitwa *majinni.* Lakini tukio linaloelezwa hapa linawahusu Mayahudi wa Nasibin ambao walikuwa wakija kufanya biashara katika soko la Okadh. Mtume *s.a.w.* alikwenda kuhubiri Taif lakini watu wa humo wakamfukuza. Njiani mahali panapoitwa Nakhla, Mtume *s.a.w.* akakutana na Mayahudi hao wa Nasibin. Basi asubuhi alipokuwa anasali wakasikia anasoma Qur'an. Nyoyo zao zikalainika, wakaingia Uislamu, na wakafikisha habari za Uislamu makwao.

وَّاَنَّهٗ كَانَ رِجَالٌ مِّنَ الْاِنْسِ يَعُوْذُوْنَ
بِرِجَالٍ مِّنَ الْجِنِّ فَزَادُوْهُمْ رَهَقًا ۙ﴿۷﴾

7. Na hakika kulikuwa na watu miongoni mwa wanadamu wakijikinga kwa watu miongoni mwa majinni, hivyo wakawazidishia kiburi:

وَّاَنَّهُمْ ظَنُّوْا كَمَا ظَنَنْتُمْ اَنْ لَّنْ يَّبْعَثَ
اللّٰهُ اَحَدًا ۙ﴿۸﴾

8. Na kwa hakika wao walidhani kama mlivyodhani ninyi ya kuwa Allah Hatamtuma ye yote.

وَّاَنَّا لَمَسْنَا السَّمَآءَ فَوَجَدْنٰهَا مُلِئَتْ
حَرَسًا شَدِيْدًا وَّشُهُبًا ۙ﴿۹﴾

9. Nasi tuliigusa mbingu tukaiona imejaa walinzi wenye nguvu na nyota zing'aazo.

وَّاَنَّا كُنَّا نَقْعُدُ مِنْهَا مَقَاعِدَ لِلسَّمْعِ ؕ
فَمَنْ يَّسْتَمِعِ الْاٰنَ يَجِدْ لَهٗ شِهَابًا رَّصَدًا ۙ﴿۱۰﴾

10. Na hakika tulikuwa tukikaa humo katika baadhi ya makao ili kusikiliza; lakini atakayejitahidi kusikiliza sasa atakuta kimwondo kikimvizia.

وَّاَنَّا لَا نَدْرِيْٓ اَشَرٌّ اُرِيْدَ بِمَنْ فِي
الْاَرْضِ اَمْ اَرَادَ بِهِمْ رَبُّهُمْ رَشَدًا ۙ﴿۱۱﴾

11. Nasi hatujui kama shari inatakiwa kwa wale wanaokaa ardhini au Mola wao Anawatakia mwongozo.

وَّاَنَّا مِنَّا الصّٰلِحُوْنَ وَمِنَّا دُوْنَ ذٰلِكَ ؕ
كُنَّا طَرَآئِقَ قِدَدًا ۙ﴿۱۲﴾

12. Na hakika miongoni mwetu wamo wema na wengine miongoni mwetu ni kinyume cha hayo: tulikuwa njia mbalimbali:

وَّاَنَّا ظَنَنَّآ اَنْ لَّنْ نُّعْجِزَ اللّٰهَ فِي الْاَرْضِ
وَلَنْ نُّعْجِزَهٗ هَرَبًا ۙ﴿۱۳﴾

13. Nasi tulijua ya kuwa hatuwezi kumdhoofisha Allah katika nchi wala hatuwezi kumponyoka kwa kukimbia:

وَّاَنَّا لَمَّا سَمِعْنَا الْهُدٰٓى اٰمَنَّا بِهٖ ؕ
فَمَنْ يُّؤْمِنْۢ بِرَبِّهٖ فَلَا يَخَافُ بَخْسًا
وَّلَا رَهَقًا ۙ﴿۱۴﴾

14. Nasi tulipousikia mwongozo, tukauamini, basi anayemwamini Mola wake hataogopa hasara wala ubaya:

وَّاَنَّا مِنَّا الْمُسْلِمُوْنَ وَمِنَّا الْقٰسِطُوْنَ ؕ
فَمَنْ اَسْلَمَ فَاُولٰٓئِكَ تَحَرَّوْا رَشَدًا ﴿۱۵﴾

15. Nasi wamo miongoni mwetu waliosilimu na wamo miongoni mwetu wanaokengeuka; lakini aliyesilimu basi hao ndio hutafuta wema:

Aya 8. *Hatamtuma ye yote.* Toka zamani watu walikuwa wanadhani kuwa Mungu hatamtuma Nabii ye yote. Itikadi ya namna hii si mpya kwa watu. Hata Mayahudi walikubaliana ya kuwa hakuna Nabii baada ya Musa (Musallaam-su-Thabuut, uk. 170). Lakini Allah aliibatilisha kwa kuwatuma Mitume baadaye.

وَاَمَّا الْقٰسِطُوْنَ فَكَانُوْا لِجَهَنَّمَ حَطَبًا ﴿١٦﴾

16. Waama wanaokengeuka basi wamekuwa kuni za Jahanamu.

وَّ اَنْ لَّوِ اسْتَقَامُوْا عَلَى الطَّرِيْقَةِ لَاَسْقَيْنٰهُمْ مَّآءً غَدَقًا ﴿١٧﴾

17. Na kama wangalishika kwa imara njia (iliyonyooka) Tungaliwanywesha maji kwa wingi,

لِّنَفْتِنَهُمْ فِيْهِ ؕ وَمَنْ يُّعْرِضْ عَنْ ذِكْرِ رَبِّهٖ يَسْلُكْهُ عَذَابًا صَعَدًا ﴿١٨﴾

18. Ili Tuwajaribu kwa hayo. Na anayepuuza kumkumbuka Mola wake Atamsukuma kwenye adhabu ngumu:

وَّ اَنَّ الْمَسٰجِدَ لِلّٰهِ فَلَا تَدْعُوْا مَعَ اللّٰهِ اَحَدًا ﴿١٩﴾

19. Na kwa hakika misikiti yote ni ya Allah, basi msimwombe mwingine pamoja na Allah.

وَّ اَنَّهٗ لَمَّا قَامَ عَبْدُ اللّٰهِ يَدْعُوْهُ كَادُوْا يَكُوْنُوْنَ عَلَيْهِ لِبَدًا ﴿٢٠﴾ ع ١١

20. Na hakika Mtumishi wa Allah aliposimama kumwomba walikuwa karibu kumwangukia (wamwangamize).

FUNGU 2

قُلْ اِنَّمَآ اَدْعُوْا رَبِّيْ وَلَآ اُشْرِكُ بِهٖۤ اَحَدًا ﴿٢١﴾

21. Sema: Ninamwomba Mola wangu tu wala simshirikishi na ye yote.

قُلْ اِنِّيْ لَاۤ اَمْلِكُ لَكُمْ ضَرًّا وَّلَا رَشَدًا ﴿٢٢﴾

22. Sema: Kwa hakika mimi similiki kwa ajili yenu dhara wala heri.

قُلْ اِنِّيْ لَنْ يُّجِيْرَنِيْ مِنَ اللّٰهِ اَحَدٌ ۙ وَّلَنْ اَجِدَ مِنْ دُوْنِهٖ مُلْتَحَدًا ﴿٢٣﴾

23. Sema: Bila shaka hapana ye yote awezaye kunilinda na Allah, wala sitapata makao ya salama ila Kwake Yeye tu:

اِلَّا بَلٰغًا مِّنَ اللّٰهِ وَرِسٰلٰتِهٖ ؕ وَمَنْ يَّعْصِ اللّٰهَ وَرَسُوْلَهٗ فَاِنَّ لَهٗ نَارَ جَهَنَّمَ خٰلِدِيْنَ فِيْهَآ اَبَدًا ﴿٢٤﴾ؕ

24. Ila kwa kufikisha (ujumbe) utokao kwa Allah na risala Zake; na atakayemwasi Allah na Mtume Wake, basi bila shaka atapata moto wa Jahanamu, watakaa humo muda mrefu.

حَتّٰۤى اِذَا رَاَوْا مَا يُوْعَدُوْنَ فَسَيَعْلَمُوْنَ مَنْ اَضْعَفُ نَاصِرًا وَّ اَقَلُّ عَدَدًا ﴿٢٥﴾

25. Hata watakapoyaona wanayoahidiwa, ndipo watajua ni nani msaidizi dhaifu na mwenye idadi ndogo.

Aya 20. *Mtumishi wa Mungu* hapa ni Mtume Muhammad *s.a.w.* Watu waliomwangukia Mtume ili kumwangamiza, wanaotajwa hapa yumkini ni watu wa Taif.

قُلْ اِنْ اَدْرِیْۤ اَقَرِیْبٌ مَّا تُوْعَدُوْنَ اَمْ یَجْعَلُ لَهٗ رَبِّیْۤ اَمَدًا ﴿۲۵﴾

26. Sema: Sijui kama yako karibu mliyoahidiwa au Mola wangu Atayawekea muda mrefu:

عٰلِمُ الْغَیْبِ فَلَا یُظْهِرُ عَلٰی غَیْبِهٖۤ اَحَدًا ﴿۲۶﴾ۙ

27. Yu Mjuzi wa yasiyoonekana, hivyo Hamdhihirishii yeyote ghaibu zake.

اِلَّا مَنِ ارْتَضٰی مِنْ رَّسُوْلٍ فَاِنَّهٗ یَسْلُكُ مِنْۢ بَیْنِ یَدَیْهِ وَمِنْ خَلْفِهٖ رَصَدًا ﴿۲۷﴾ۙ

28. Isipokuwa Mtume Aliyemridhia. Na mbele yake na nyuma yake hutembea malaika kama walinzi.

لِّیَعْلَمَ اَنْ قَدْ اَبْلَغُوْا رِسٰلٰتِ رَبِّهِمْ وَاَحَاطَ بِمَا لَدَیْهِمْ وَاَحْصٰی كُلَّ شَیْءٍ عَدَدًا ﴿۲۸﴾ع ۲/۱۲

29. Ili Ajulishe ya kuwa wamekwisha fikisha risala za Mola wao; na Ameyazunguka waliyo nayo na Amehesabu idadi ya kila kitu.

Aya 27. *Falaa yudh-hiru 'alaa ghaibihi,* "Hamdhihirishii siri Yake." Neno dhahara lililotumiwa hapa pia maana yake ni kushinda (sura 51:10); ndiyo kusema, kumfanya mtu apate ushindi juu ya siri zile, yaani azipate kwa wingi. Watu wengi wanaonyeshwa siri kidogo kidogo katika njozi na ndoto, lakini Manabii hupewa kwa wingi kabisa. Hivyo anayefunuliwa na Allah mambo ya ghaibu kwa wingi sana huwa Nabii Wake.

Biblia inasema kwamba mtu asemaye neno kwa jina la Allah nalo likafanyika vile alivyosema, yu mkweli (Kumbukumbu 18:22).

سُوْرَةُ الْمُزَّمِّلِ مَكِّيَّةٌ وَّ هِيَ مَعَ الْبَسْمَلَةِ اِحْدٰى وَ عِشْرُوْنَ اٰيَةً وَّ رُكُوْعَانِ

73. SURA AL-MUZZAMMIL

Imeteremshwa Makka

Ina mafungu 2 na Aya 21 pamoja na Bismillahi

بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ ①

1. Kwa jina la Allah, Mwingi wa rehema, Mwingi wa ukarimu.

يٰۤاَيُّهَا الْمُزَّمِّلُ ۙ②

2. Ewe uliyejifunika nguo!

قُمِ الَّيْلَ اِلَّا قَلِيْلًا ۙ③

3. Simama usiku ila kidogo,

نِّصْفَهٗۤ اَوِ انْقُصْ مِنْهُ قَلِيْلًا ۙ④

4. Nusu yake au ipunguze kidogo,

اَوْ زِدْ عَلَيْهِ وَرَتِّلِ الْقُرْاٰنَ تَرْتِيْلًا ۚ⑤

5. Au izidishe na soma Qur'an kwa vizuri.

اِنَّا سَنُلْقِيْ عَلَيْكَ قَوْلًا ثَقِيْلًا ⑥

6. Hakika Sisi hivi karibuni Tutakuteremshia kauli nzito.

اِنَّ نَاشِئَةَ الَّيْلِ هِيَ اَشَدُّ وَطْـًٔا وَّاَقْوَمُ قِيْلًا ؕ⑦

7. Hakika kuamka usiku ni (njia) bora zaidi kwa kuikanyaga (nafsi) na vizuri zaidi kutamka.

اِنَّ لَكَ فِي النَّهَارِ سَبْحًا طَوِيْلًا ؕ⑧

8. Hakika mchana kwako una shughuli nyingi.

وَاذْكُرِ اسْمَ رَبِّكَ وَ تَبَتَّلْ اِلَيْهِ تَبْتِيْلًا ؕ⑨

9. Na likumbuke jina la Mola wako na ujitupe Kwake kwa kujitupa hasa.

Jina la sura hii linatoka katika Aya ya 2 Mtume *s.a.w.* anapoitwa aliyejifunika.

Sura hii ilishuka Makka na wafasiri wanaifikiria kuwa ni katika sura za mwanzo kushuka. Wengi wanasema ya kuwa Aya ya mwisho ya sura hii ilishuka Madina.

Aya 2. *Uliyejifunika.* Aliyejifunika ni Mtume *s.a.w.* Alipopata ufunuo wa kwanza uliomwamrisha kushika kazi ya kuhubiria watu dini mpya, Mtume *s.a.w.*, kwa kuona uzito wa kazi aliyopewa akaona hofu, na akarudi nyumbani akawaambia wamfunike. Katika Aya hizi Allah anamwambia ya kuwa kwa kufanya kazi hiyo vizuri anatakiwa afanye bidii kumwomba Allah na kusoma Qur'an.

Aya 6. Kauli nzito, ni wahyi ulioshuka ili kumpa amri ya kuusuluhisha ulimwengu nzima, hii bila shaka ilikuwa kauli nzito, na kazi ngumu.

رَبُّ الْمَشْرِقِ وَالْمَغْرِبِ لَآ اِلٰهَ اِلَّا هُوَ فَاتَّخِذْهُ وَكِيْلًا ۝١٠

10. (Yeye ni) Mola wa mashariki na magharibi hakuna mwabudiwa ila Yeye, basi Umfanye kuwa Mlinzi.

وَاصْبِرْ عَلٰى مَا يَقُوْلُوْنَ وَاهْجُرْهُمْ هَجْرًا جَمِيْلًا ۝١١

11. Na fanya subira juu ya hayo wayasemayo na utengane nao kwa namna nzuri.

وَذَرْنِيْ وَالْمُكَذِّبِيْنَ اُولِي النَّعْمَةِ وَمَهِّلْهُمْ قَلِيْلًا ۝١٢

12. Na Niache Mimi na wanaokadhibisha walioneemeka, na uwape muhula kidogo.

اِنَّ لَدَيْنَآ اَنْكَالًا وَّجَحِيْمًا ۝١٣

13. Hakika Tunazo pingu na Moto uwakao.

وَّطَعَامًا ذَا غُصَّةٍ وَّعَذَابًا اَلِيْمًا ۝١٤

14. Na chakula kikwamacho kooni na adhabu iumizayo.

يَوْمَ تَرْجُفُ الْاَرْضُ وَالْجِبَالُ وَكَانَتِ الْجِبَالُ كَثِيْبًا مَّهِيْلًا ۝١٥

15. Siku ardhi na milima vitakapotetemeka, na milima itakuwa kama lundo la mchanga linalosambaa.

اِنَّآ اَرْسَلْنَآ اِلَيْكُمْ رَسُوْلًا شَاهِدًا عَلَيْكُمْ كَمَآ اَرْسَلْنَآ اِلٰى فِرْعَوْنَ رَسُوْلًا ۝١٦

16. Hakika Sisi Tumewatumieni Mtume aliye shahidi juu yenu, kama Tulivyompeleka Mtume kwa Firauni.

فَعَصٰى فِرْعَوْنُ الرَّسُوْلَ فَاَخَذْنٰهُ اَخْذًا وَّبِيْلًا ۝١٧

17. Lakini Firauni alimwasi Mtume, basi Tukamkamata mkamato wa mashaka.

فَكَيْفَ تَتَّقُوْنَ اِنْ كَفَرْتُمْ يَوْمًا يَّجْعَلُ الْوِلْدَانَ شِيْبًا ۝١٨

18. Basi ninyi mkikufuru mtawezaje kujikinga dhidi ya siku itakayowafanya watoto kuwa wazee?

السَّمَآءُ مُنْفَطِرٌ بِهٖ كَانَ وَعْدُهٗ مَفْعُوْلًا ۝١٩

19. Mbingu zitapasuka kwayo; ahadi Yake itakuwa imetimizwa.

اِنَّ هٰذِهٖ تَذْكِرَةٌ فَمَنْ شَآءَ اتَّخَذَ اِلٰى رَبِّهٖ سَبِيْلًا ۝٢٠

20. Kwa hakika huu ni ukumbusho, basi anayetaka ashike njia kwa Mola wake.

Aya 16. Mtume *s.a.w.* hapa amefananishwa na Nabii Musa. Na historia inaonyesha ya kuwa Manabii hawa wawili wamefanana sana. Nabii Musa alipewa Sheria mpya na Nabii Muhammad pia akapewa Sheria mpya. Wote wawili walipigana vita na maadui zao. Na kama vile walivyofika Makhalifa baada ya Nabii Musa, kadhalika walifika Makhalifa baada ya Mtume *s.a.w.* Na kama vile alivyofika Masihi baada ya miaka 1,300 baada ya Nabii Musa, kadhalika aliahidiwa kufika Masihi kwa Waislamu miaka 1,300 baada ya Mtume Muhammad *s.a.w.,* naye amekwisha fika, Seyidna Ahmad *(alaihissalaam),* na hivyo mfano uliotajwa hapa umekamilika.

FUNGU 2

21. Kwa hakika Mola wako Anajua kuwa wewe husimama (kumwabudu) karibu na thuluthi mbili za usiku, pengine nusu yake, au thuluthi yake, na (pia) baadhi ya watu walio pamoja nawe; na Allah Huupima usiku na mchana. Anajua kuwa hamwezi kufanya hivyo, basi Amewaelekeeni kwa rehema, kwa hiyo someni yaliyo rahisi katika Qur'an. Anajua ya kuwa baadhi yenu watakuwa wagonjwa na wengine watasafiri katika ardhi wakiitafuta fadhili ya Allah, na wengine watapigana katika njia ya Allah, kwa hiyo someni yaliyo rahisi humo. Na simamisheni Sala na toeni Zaka, na Mkatieni Allah sehemu njema, na heri yo yote mnayotanguliza kwa ajili ya nafsi zenu mtaipata kwa Allah; Yeye ni Mbora na Mkubwa wa (kulipa) ujira; na ombeni msamaha kwa Allah; hakika Allah ni Msamehevu, Mwingi wa Ukarimu.

اِنَّ رَبَّكَ يَعْلَمُ اَنَّكَ تَقُوْمُ اَدْنٰى مِنْ ثُلُثَيِ
الَّيْلِ وَنِصْفَهٗ وَثُلُثَهٗ وَطَآئِفَةٌ مِّنَ الَّذِيْنَ
مَعَكَ ؕ وَاللّٰهُ يُقَدِّرُ الَّيْلَ وَالنَّهَارَ ؕ عَلِمَ اَنْ
لَّنْ تُحْصُوْهُ فَتَابَ عَلَيْكُمْ فَاقْرَءُوْا مَا
تَيَسَّرَ مِنَ الْقُرْاٰنِ ؕ عَلِمَ اَنْ سَيَكُوْنُ مِنْكُمْ
مَّرْضٰى ۙ وَاٰخَرُوْنَ يَضْرِبُوْنَ فِى الْاَرْضِ
يَبْتَغُوْنَ مِنْ فَضْلِ اللّٰهِ ۙ وَاٰخَرُوْنَ
يُقَاتِلُوْنَ فِىْ سَبِيْلِ اللّٰهِ ۖ فَاقْرَءُوْا مَا تَيَسَّرَ
مِنْهُ ۙ وَاَقِيْمُوا الصَّلٰوةَ وَاٰتُوا الزَّكٰوةَ
وَاَقْرِضُوا اللّٰهَ قَرْضًا حَسَنًا ؕ وَمَا تُقَدِّمُوْا
لِاَنْفُسِكُمْ مِّنْ خَيْرٍ تَجِدُوْهُ عِنْدَ اللّٰهِ هُوَ
خَيْرًا وَّاَعْظَمَ اَجْرًا ؕ وَاسْتَغْفِرُوا اللّٰهَ ؕ
اِنَّ اللّٰهَ غَفُوْرٌ رَّحِيْمٌ ﴿٢١﴾ ع ٢

سُوْرَةُ الْمُدَّثِّرِ مَكِّيَّةٌ وَّ هِيَ مَعَ الْبَسْمَلَةِ سَبْعٌ وَّ خَمْسُوْنَ اٰيَةً وَّ رُكُوْعَانِ

74. SURA AL-MUDDATHTHIR

Imeteremshwa Makka

Ina mafungu 2 na Aya 57 pamoja na Bismillahi

بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ ①

1. Kwa jina la Allah, Mwingi wa rehema, Mwingi wa ukarimu.

يٰۤاَيُّهَا الْمُدَّثِّرُ ۙ②

2. Ewe uliyevaa.

قُمْ فَاَنْذِرْ ۖۗ③

3. Simama na uonye.

وَ رَبَّكَ فَكَبِّرْ ۖۗ④

4. Na Mola wako umtukuze.

وَ ثِيَابَكَ فَطَهِّرْ ۖۗ⑤

5. Na nguo zako uzitakase.

وَ الرُّجْزَ فَاهْجُرْ ۖۗ⑥

6. Na uchafu uuondoe.

وَ لَا تَمْنُنْ تَسْتَكْثِرُ ۖۗ⑦

7. Wala usiwafanyie ihsani ili upate zaidi.

وَ لِرَبِّكَ فَاصْبِرْ ؕ⑧

8. Na kwa ajili ya Mola wako fanya subira.

Sura iliyotangulia inamweleza Mtume s.a.w. namna ya kufikia ukamilifu. Sura hii inamwamuru atoke faraghani na kuwakamilisha watu wengine. Wafasiri wote wanakubali ya kuwa sura hii ndiyo ya pili kushuka. Ni dhahiri sura hii nzima haikushuka yote mara moja; nayo ilishuka Makka.

Aya 2. *Muddaththir,* "Uliyevaa." *Dithaar* ni nguo anayovaa mtu juu ya nguo zingine, kama shuka kubwa au blanketi.

Aya 5. Neno *thiyaabaka* laweza kuwa na maana ya moyo lakini iwapo tu kama litachukuliwa kimethali. Lakini tatizo lake ni kwamba neno *thiyaab* kwa tafsiri ya neno kwa neno lina maana ya nguo au mavazi. Kwa hiyo kama mtu atalichukulia kimethali moyo hautakuwa tafsiri pekee inayowezekana. Inawezekana sana kwamba pengine *thiyaabaka* katika maudhui hii laweza kuwa linawarejea masahaba wa Mtukufu Mtume s.a.w., na watu wengine walio karibu naye. Hivyo basi tafsiri ya pili iliyopendekezwa ni ya neno kwa neno inayompatia msomaji uchaguzi mpana zaidi wa kutafsiri.

Aya 6. *Na uchafu uuondoe.* Neno *rujz* (uchafu) lililotumiwa hapa pia maana yake ni wasiwasi, na upinzani. Ndiyo kusema, Mtume s.a.w. anaambiwa asijali upinzani wa watu wala asipate hofu, na pia awafunze watu usafi na kuondoa uchafu.

فَاِذَا نُقِرَ فِي النَّاقُوْرِ ۙ﴿٨﴾

9. Basi itakapopigwa tarumbeta,

فَذٰلِكَ يَوْمَئِذٍ يَّوْمٌ عَسِيْرٌ ۙ﴿٩﴾

10. Basi siku hiyo itakuwa Siku ngumu,

عَلَى الْكٰفِرِيْنَ غَيْرُ يَسِيْرٍ ﴿١٠﴾

11. Kwa makafiri haitakuwa nyepesi.

ذَرْنِيْ وَمَنْ خَلَقْتُ وَحِيْدًا ۙ﴿١١﴾

12. Uniache Mimi na Niliyemwumba Peke Yangu,

وَّجَعَلْتُ لَهٗ مَالًا مَّمْدُوْدًا ۙ﴿١٢﴾

13. Na Nikamjaalia mali nyingi,

وَّبَنِيْنَ شُهُوْدًا ۙ﴿١٣﴾

14. Na watoto waonekanao,

وَّمَهَّدْتُّ لَهٗ تَمْهِيْدًا ۙ﴿١٤﴾

15. Na nikampangia mpango;

ثُمَّ يَطْمَعُ اَنْ اَّزِيْدَ ۖ﴿١٥﴾

16. Kisha anatumaini Nizidishe!

كَلَّا ؕ اِنَّهٗ كَانَ لِاٰيٰتِنَا عَنِيْدًا ؕ﴿١٦﴾

17. Siyo! Hakika yeye alikuwa adui wa Ishara Zetu.

سَاُرْهِقُهٗ صَعُوْدًا ؕ﴿١٧﴾

18. Karibuni Nitamtesa kwa mateso makuu.

اِنَّهٗ فَكَّرَ وَقَدَّرَ ۙ﴿١٨﴾

19. Hakika yeye alitafakari na alikadiria.

فَقُتِلَ كَيْفَ قَدَّرَ ۙ﴿١٩﴾

20. Basi aangamizwe, alikadiriaje!

ثُمَّ قُتِلَ كَيْفَ قَدَّرَ ۙ﴿٢٠﴾

21. Tena aangamizwe alikadiriaje!

ثُمَّ نَظَرَ ۙ﴿٢١﴾

22. Kisha akatazama,

ثُمَّ عَبَسَ وَبَسَرَ ۙ﴿٢٢﴾

23. Kisha alikunja kipaji na akafinya uso,

ثُمَّ اَدْبَرَ وَاسْتَكْبَرَ ۙ﴿٢٣﴾

24. Kisha aligeuka na akajivuna.

فَقَالَ اِنْ هٰذَاۤ اِلَّا سِحْرٌ يُّؤْثَرُ ۙ﴿٢٤﴾

25. Na akasema: Huu si kitu ila ni uchawi ulionukuliwa;

اِنْ هٰذَاۤ اِلَّا قَوْلُ الْبَشَرِ ؕ﴿٢٥﴾

26. Hii siyo ila ni kauli ya binadamu.

سَاُصْلِيْهِ سَقَرَ ﴿٢٦﴾

27. Karibuni Nitamtupa katika 'saqar'

وَمَاۤ اَدْرٰىكَ مَا سَقَرُ ؕ﴿٢٧﴾

28. Na nini kitakujulisha 'saqar' ni kitu gani?

لَا تُبْقِيْ وَلَا تَذَرُ ﴿٢٩﴾

29. Hautabakisha chochote na wala hautaacha (nyuma) chochote.

لَوَّاحَةٌ لِّلْبَشَرِ ﴿٣٠﴾

30. Huiunguza ngozi.

عَلَيْهَا تِسْعَةَ عَشَرَ ﴿٣١﴾

31. Juu yake wako (walinzi) kumi na tisa,

وَمَا جَعَلْنَآ اَصْحٰبَ النَّارِ اِلَّا مَلٰٓئِكَةً ۙ وَّمَا جَعَلْنَا عِدَّتَهُمْ اِلَّا فِتْنَةً لِّلَّذِيْنَ كَفَرُوْا ۙ لِيَسْتَيْقِنَ الَّذِيْنَ اُوْتُوا الْكِتٰبَ وَيَزْدَادَ الَّذِيْنَ اٰمَنُوْٓا اِيْمَانًا وَّلَا يَرْتَابَ الَّذِيْنَ اُوْتُوا الْكِتٰبَ وَالْمُؤْمِنُوْنَ ۙ وَلِيَقُوْلَ الَّذِيْنَ فِيْ قُلُوْبِهِمْ مَّرَضٌ وَّالْكٰفِرُوْنَ مَاذَآ اَرَادَ اللّٰهُ بِهٰذَا مَثَلًا ۭ كَذٰلِكَ يُضِلُّ اللّٰهُ مَنْ يَّشَاۗءُ وَيَهْدِيْ مَنْ يَّشَاۗءُ ۭ وَمَا يَعْلَمُ جُنُوْدَ رَبِّكَ اِلَّا هُوَ ۭ وَمَا هِيَ اِلَّا ذِكْرٰى لِلْبَشَرِ ﴿٣١﴾ ع ۝١٥

32. Na Hatukuwaweka walinzi wa Moto ila Malaika, wala Hatukuifanya hesabu yao ila kuwa jaribio kwa wale waliokufuru, ili wawe na yakini waliopewa Kitabu, na walioamini wazidi katika imani, wala wasiwe na shaka wale waliopewa Kitabu na waaminio, na ili walio na ugonjwa katika mioyo yao na waliokufuru waseme: Anataka nini Allah kwa mfano huu? Hivyo Allah Humwacha kupotea Amtakaye na Humwongoza Amtakaye, wala hapana ye yote ajuaye majeshi ya Mola wako ila Yeye tu; na hayo si kitu ila ni ukumbusho kwa mwanadamu.

FUNGU 2

كَلَّا وَالْقَمَرِ ﴿٣٢﴾

33. Sivyo! Naapa kwa mwezi,

وَالَّيْلِ اِذْ اَدْبَرَ ﴿٣٣﴾

34. Na kwa usiku unapokucha,

وَالصُّبْحِ اِذَآ اَسْفَرَ ﴿٣٤﴾

35. Na kwa asubuhi inapopambazuka:

اِنَّهَا لَاِحْدَى الْكُبَرِ ﴿٣٥﴾

36. Hakika huo ni mmojawapo katika misiba mikubwa,

نَذِيْرًا لِّلْبَشَرِ ﴿٣٦﴾

37. Ni onyo kwa binadamu,

لِمَنْ شَاۗءَ مِنْكُمْ اَنْ يَّتَقَدَّمَ اَوْ يَتَاَخَّرَ ﴿٣٧﴾

38. Kwa anayetaka miongoni mwenu kutakadamu au kutaakhari.

كُلُّ نَفْسٍۢ بِمَا كَسَبَتْ رَهِيْنَةٌ ﴿٣٨﴾

39. Kila nafsi ni rehani kwa iliyoyachuma,

اِلَّآ اَصْحٰبَ الْيَمِيْنِ ﴿٣٩﴾

40. Isipokuwa watu wa kulia.

فِيْ جَنّٰتٍ ۛ يَتَسَآءَلُوْنَ ۙ﴿٤١﴾ عَنِ الْمُجْرِمِيْنَ ۙ﴿٤٢﴾ مَا سَلَكَكُمْ فِيْ سَقَرَ ﴿٤٣﴾ قَالُوْا لَمْ نَكُ مِنَ الْمُصَلِّيْنَ ۙ﴿٤٤﴾ وَلَمْ نَكُ نُطْعِمُ الْمِسْكِيْنَ ۙ﴿٤٥﴾ وَكُنَّا نَخُوْضُ مَعَ الْخَآئِضِيْنَ ۙ﴿٤٦﴾ وَكُنَّا نُكَذِّبُ بِيَوْمِ الدِّيْنِ ۙ﴿٤٧﴾ حَتّٰٓى اَتٰىنَا الْيَقِيْنُ ﴿٤٨﴾ فَمَا تَنْفَعُهُمْ شَفَاعَةُ الشّٰفِعِيْنَ ﴿٤٩﴾ فَمَا لَهُمْ عَنِ التَّذْكِرَةِ مُعْرِضِيْنَ ۙ﴿٥٠﴾ كَاَنَّهُمْ حُمُرٌ مُّسْتَنْفِرَةٌ ۙ﴿٥١﴾ فَرَّتْ مِنْ قَسْوَرَةٍ ﴿٥٢﴾ بَلْ يُرِيْدُ كُلُّ امْرِئٍ مِّنْهُمْ اَنْ يُّؤْتٰى صُحُفًا مُّنَشَّرَةً ۙ﴿٥٣﴾ كَلَّا ۭ بَلْ لَّا يَخَافُوْنَ الْاٰخِرَةَ ﴿٥٤﴾ كَلَّآ اِنَّهٗ تَذْكِرَةٌ ۚ﴿٥٥﴾ فَمَنْ شَآءَ ذَكَرَهٗ ﴿٥٦﴾ وَمَا يَذْكُرُوْنَ اِلَّآ اَنْ يَّشَآءَ اللّٰهُ ۭ هُوَ اَهْلُ التَّقْوٰى وَاَهْلُ الْمَغْفِرَةِ ﴿٥٧﴾ ع ۝

41. Katika Mabustani wataulizana,
42. Juu ya wakosefu:
43. Na nini kilichowapelekeni katika 'saqar'?
44. Watasema: Hatukuwa miongoni mwa wanaosali,
45. Wala hatukuwa tukilisha maskini,
46. Na tulikuwa tukipiga porojo pamoja na wapigao porojo,
47. Na tulikuwa tukikadhibisha Siku ya hukumu,
48. Mpaka mauti yakatufika.
49. Basi hautawafaa uombezi wa waombezi.
50. Basi wamekuwaje kukengeuka onyo hili.
51. Kana kwamba ni mapunda wenye kushtuka,
52. Wanaomkimbia simba?
53. Bali! Kila mmoja wao anataka apewe nyaraka zilizofunuliwa.
54. Sivyo, bali wao hawaiogopi Akhera.
55. Tahadhari! kwa hakika hiyo ni nasaha kubwa.
56. Basi anayetaka aikumbuke.
57. Na hawatakumbuka isipokuwa Apende Allah; Yeye ndiye Mwenye kuogopwa na Mwenye kusamehe.

Aya 44. *Hatukuwa miongoni mwa waliosali.* Haya ndiyo majibu ya watu watakaotiwa Motoni, ya kwamba hawakuwa wanaosali, hawakuwa wanawalisha maskini, na walikuwa wakipiga porojo na kuikadhibisha Siku ya Kiyama. hapa pana somo jema kwa ajili ya Waislamu kukumbuka.

سُوْرَةُالْقِيَامَةِ مَكِّيَّةٌ وَّ هِيَ مَعَ الْبَسْمَلَةِ اِحْدٰى وَ اَرْبَعُوْنَ اٰيَةً وَّ رُكُوْعَانِ

75. SURA AL-QIYAAMA

Imeteremshwa Makka

Ina mafungu 2 na Aya 41 pamoja na Bismillahi

بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ ①

1. Kwa jina la Allah, Mwingi wa rehema, Mwingi wa ukarimu.

لَآ اُقْسِمُ بِيَوْمِ الْقِيٰمَةِ ۙ ②

2. Naapa kwa siku ya Kiyama.

وَلَآ اُقْسِمُ بِالنَّفْسِ اللَّوَّامَةِ ؕ ③

3. Na naapa pia kwa nafsi inayojilaumu (mno).

اَيَحْسَبُ الْاِنْسَانُ اَلَّنْ نَّجْمَعَ عِظَامَهٗ ؕ ④

4. Je, mtu anafikiri ya kuwa Sisi Hatutaikusanya mifupa yake?

بَلٰى قٰدِرِيْنَ عَلٰٓى اَنْ نُّسَوِّيَ بَنَانَهٗ ⑤

5. Naam! Tunaweza (hata) kuzisawazisha ncha za vidole vyake.

بَلْ يُرِيْدُ الْاِنْسَانُ لِيَفْجُرَ اَمَامَهٗ ۚ ⑥

6. Lakini mtu anataka aendelee kufanya dhambi mbele Yake.

يَسْـَٔلُ اَيَّانَ يَوْمُ الْقِيٰمَةِ ؕ ⑦

7. Anauliza: Itakuwa lini siku ya Kiyama?

فَاِذَا بَرِقَ الْبَصَرُ ۙ ⑧

8. Basi jicho litakapofanya kiwi,

وَخَسَفَ الْقَمَرُ ۙ ⑨

9. Na mwezi utakapopatwa,

وَجُمِعَ الشَّمْسُ وَالْقَمَرُ ۙ ⑩

10. Na jua na mwezi vitakapokutanishwa (katika kupatwa),

Sura hii inaendeleza habari iliyoelezwa mwisho wa sura iliyotangulia ya kwamba Qur'an ni kumbukumbu itakayowainua na kuwapa cheo wanaoifuata. Kuhakikisha jambo hili siku ya kufufuka, ambayo ndiyo jina la sura hii, na nafsi inayojilaumu vinatolewa kuwa ushahidi ya kwamba wanaofuata Uislamu watakuwa kama waliokufa ambao wamefufuka na kutukuka sana. Sura hii ilishuka Makka.

Aya 3. *Nafsi al-Lawwaamah* ni nafsi inayojilaumu. Kwa ajili ya maendeleo ya kiroho Qur'an imeeleza madaraja matatu: (1) *Nafsi ammaara* (sura 12:54), yaani nafsi inayomwelekeza mtu maovuni na kutaka kumwongoza katika mabaya matupu na kumzuia asiufikie wema mkamilifu; (2) *Nafsi al-lawwaamah* (sura 75:3), yaani roho ile inayojilaumu kila inapolegea kuyatenda yaipasayo, au inapoasi japo katika jambo lililo dogo, mara inatambua yenyewe ukosaji wake; inapozoea katika daraja hii na kuzidi kukua inafikia daraja ya (3) inayoitwa *Nafsi al-mutmainnah* (sura) 89:28-31) yaani roho iliyopumzika, isiyo na udhaifu wala upungufu, na inatiwa nguvu na kuungana hasa na Allah na haiwi radhi kuishi pasipo Yeye. Habari zaidi juu ya jambo hili someni kitabu "Uislamu na Hekima yake."

يَقُوْلُ الْاِنْسَانُ يَوْمَئِذٍ اَيْنَ الْمَفَرُّ ﴿١١﴾

11. Mtu atasema siku hiyo: Pa wapi mahali pa kukimbilia?

كَلَّا لَا وَزَرَ ﴿١٢﴾

12. La, hakuna mahali pa kukimbilia.

اِلٰى رَبِّكَ يَوْمَئِذِ ِالْمُسْتَقَرُّ ﴿١٣﴾

13. Siku hiyo patakuwa kwa Mola wako mahali pa kustarehe.

يُنَبَّؤُا الْاِنْسَانُ يَوْمَئِذٍ بِمَا قَدَّمَ وَاَخَّرَ ﴿١٤﴾

14. Siku hiyo mtu ataambiwa aliyoyatanguliza na aliyoyakawiza.

بَلِ الْاِنْسَانُ عَلٰى نَفْسِهٖ بَصِيْرَةٌ ﴿١٥﴾

15. Bali mtu anaijua vizuri sana nafsi yake.

وَّلَوْ اَلْقٰى مَعَاذِيْرَهٗ ﴿١٦﴾

16. Ingawa atoe udhuru wake wa uwongo,

لَا تُحَرِّكْ بِهٖ لِسَانَكَ لِتَعْجَلَ بِهٖ ﴿١٧﴾

17. Usiutikisie (ufunuo) ulimi wako kwa kuufanyia haraka,

اِنَّ عَلَيْنَا جَمْعَهٗ وَقُرْاٰنَهٗ ﴿١٨﴾

18. Kwa hakika ni juu Yetu kuukusanya na kuusomesha.

فَاِذَا قَرَاْنٰهُ فَاتَّبِعْ قُرْاٰنَهٗ ﴿١٩﴾

19. Hivyo Tutakapousoma, basi fuata kusomwa kwake.

ثُمَّ اِنَّ عَلَيْنَا بَيَانَهٗ ﴿٢٠﴾

20. Kisha ni juu Yetu kuubainisha.

كَلَّا بَلْ تُحِبُّوْنَ الْعَاجِلَةَ ﴿٢١﴾

21. Tahadhari! Bali ninyi mnaipenda dunia.

Aya 17-20. Mtume Muhammad *s.a.w.* alikuwa na hamu sana ya kuyakumbuka maneno ya wahyi. Allah alimtuliza moyo akamchukulia kazi yote ya (i) kuyakusanya, (ii) ya kusomwa kwake Qur'an na (iii) ya kueleza maneno yake. Kazi hizo tatu zilizo muhimu sana zikafanywa kwa njia ya kustaajabisha mno:-

(1) Mtume alipofunuliwa tu sehemu yo yote ya Qur'an alikuwa anamwita mwandishi wake kumwandikisha maneno yote yaliyofunuliwa. Kwani yeye mwenyewe hakujua kuandika wala kusoma. Akienda safari alikuwa anamchukua mwandishi wake kuenda pamoja naye. Ikaendelea hivyo mpaka Aya 5:4 iliposhuka na ikanadi kwamba Sheria imekamilika.

(2) Aya za Qur'an zilishushwa kidogo kidogo kadiri ilivyohitajika. Sura fupi zilitangulia kuteremshwa nazo zikaeleza umoja wa Mungu, malipo ya waaminio na makafiri katika Akhera, maagizo ya kuwahurumia maskini na mayatima na amri ya kuwapa uhuru watumwa. Waislamu waliambiwa kwamba hawana budi kuteswa na maadui kama nyimati za Manabii wa zamani walivyoteswa lakini mwishowe watafuzu na dini yao itastawi. Sura zilizofuata zilibainisha mafundisho mengine yatakiwayo kuikamilisha Sheria, na majibu ya hoja za makafiri, na bishara za Qur'an na zile za Manabii wa kale zilizotimia. Sura zote pamoja na Aya zao zilipangwa kwa taratibu hii tuliyo nayo kwa amri ya Mtume *s.a.w.*

(3) Mtume *s.a.w.* alipofariki aliwaachia masahaba wake sura zote hali zimekwisha andikwa vipande vipande juu ya vitu mbalimbali. Qur'an ilikusanywa iwe chuo kimoja katika siku za Seyidna Abu Bakar, ambaye alikuwa Khalifa wa Kwanza.

(4). Kulikuwa makabila mengi ya Waarabu, waliohitilafiana wenyewe kwa wenyewe katika matamko mengine au kuviita vitu vingine kwa majina mengine, kama tuonavyo Kiunguja, Kimrima, Kimvita na Kiamu katika nchi hii ya Afrika Mashariki. Qur'an ilifunuliwa katika lugha ya ki-Hijazi, lakini, mwanzoni watu waliruhusiwa kuisoma kwa mwafaka wa kikwao. Tofauti ya matamko yao ilikuwa kama ya *nti* na *nchi, njia* na *ndia* na kadhalika. Katika zama za Khalifa wa Tatu, Seyidna Uthman, Qur'an iliandikwa na kutangazwa kwa mwafaka wa ki-Hijaz tu, na kuisoma vingine kukapigwa marufuku. Seyidna Uthman aliufuatisha tu ule msahafu wa asili uliokusanywa na Khalifa wa Kwanza, ambao bibi Hafsa, mkewe Mtume *s.a.w.* alikuwa nao. Hakuongeza wala kupunguza cho chote. Ndiyo maana kusema ya kuwa yote yaliyomo katika misahafu ya siku hizi ni maneno ya Allah hasa.

(5) Waarabu wa zamani walijulikana sana kwa ajili ya kumbuko lao zuri. Huenda mtu mmoja alikumbuka mashairi elfu kumi ya washairi wa zamani. Allah aliwachagua watu hao wawe walinzi wa kwanza wa Neno Lake. Mtume *s.a.w.* alipoteremshiwa Aya yo yote ya Qur'an, mbali na kuiandikisha kwa waandishi wake, aliikumbuka na masahaba zake pia waliikumbuka. Sura za Qur'an ziliteremka vipande-vipande na hivyo ikawa rahisi sana kuzikumbuka. Hata mshuko wa Qur'an ulipokwisha kulikwisha patikana watu mamia na mamia walioijua Qur'an kwa moyo. Huu ndio mwujiza wenye shani uliotendeka katika nchi ya Waarabu. Palikuwa na masahaba waliomaliza juzu zote thelathini kwa moyo katika usiku mmoja.

Mtume *s.a.w.* aliwahimiza kukumbuka Qur'an sana. Alichagua watu wengine walioelewa sana kuisoma kwa ghaibu akawapeleka nchi nyingine ambako walisilimu watu ili kuwafunza wapate kuikumbuka vile vile. Desturi ya kuhifadhi Qur'an kwa njia hii ya ajabu ikaendelea hata sasa. Miji mingi ya Waislamu ina watu waisomao kwa moyo Qur'an nzima. Kila Mwislamu amewajibishwa kuzikumbuka Aya chache ama sura chache kuzisoma katika sala zake za kawaida. Katika mwezi wa Ramadhani Waislamu hukusanyika na kusomewa Qur'an nzima na watu waijuao kwa ghaibu. Ndivyo ilivyofanyika ili uwe ushuhuda ulio wazi ya kuwa Qur'an ni Sheria ya daima.

(6) Nakala za misahafu zilipelekwa na Waislamu kwa upesi sana katika kila nchi Uislamu ulikofika. Na hivyo ikawa vigumu kugeuza neno lo lote katika misahafu ya nchi fulani.

(7) Hitilafu ilitokea baina ya Waislamu katika wakati wa Seyidna Ali, nao wakagawanyika katika makundi matatu - Wasunni; Wakharji na Washia, nao wote wakaishikilia Qur'an. Hitilafu hiyo tena ikawa sababu mojawapo ya kuilinda Qur'an. Maana, watu wa kundi moja wangejaribu kuibadili maneno yake, kundi jingine lingewalaumu kufanya mageuzi ya neno la Mungu.

Qur'an ndicho chuo cha pekee katika vyuo vyote vya dini kisomwacho na watu mamilioni katika lugha yake ile ile ya asili. Waislamu wengi, wake kwa waume, watoto kwa wazee, huisoma kila siku ili kubarikiwa na maneno yake na kupata thawabu.

Maulamaa na Mafukahaa na Maimamu wanaisoma ili wapate nuru na uongofu na dalili za kushindania na maadui.

WasioWaislamu wanaisoma kwa kujua mafundisho yake au kutafuta hoja za kuwapinga Waislamu. Basi kusomwa kwa Qur'an kunafanyika kwa namna isiyo na mfano.

Maneno ya Qur'an yamehifadhiwa kwa njia isiyoweza kufikiriwa yahifadhiwe zaidi ya hapo. Lakini maneno yenyewe huwa mbali na maelezo yao. Sheria iko barabara lakini wafuasi ndio wanaitupilia mbali au kuifasiri vibaya, kama Mayahudi walivyoifanya Biblia. Qur'an haikuachwa ovyo. Mwanzoni Mtume *s.a.w.* mwenyewe alikuwa mwalimu mkuu mwenye kufichua maana za ndani za ufunuo wake, kwa sababu Qur'an iliwekwa amana kifuani mwake. Hapana ye yote awezaye kuieleza vizuri kuliko yeye. yote aliyotamka hupatikana katika vitabu vya Hadithi zake. Baadaye wakaondokea maimamu na mafukahaa wakaihudumu kadiri walivyoweza. Mtume mwenyewe alisema, "Allah atasimamisha katika umati huu mtu wa kujadidisha dini katika mwanzo wa kila karne." (Abu Dawud). Vile vile alisema, "Hakutakosa taifa moja katika umati wangu watakaoendelea kupigania haki mpaka siku ya Kiyama." Kwa mwafaka wa ahadi hii Allah amemtuma Seyidna Ahmad wa Kadiani katika siku hizi kuitilia nguvu dini ya Kiislamu. Ndivyo itakavyokuwa siku zote hata ijapo siku ya mwisho.

Kudhani ya kwamba Aya fulani za Qur'an zimefutwa na nyingine, kumebatilishwa na Qur'an (sura 41:42, 43). Kifutwacho hakihifadhiwi. Ni watu wenye bahati nzuri namna gani waifuatao Sheria inayohifadhiwa maana zake na maneno yake hata milele!

وَتَذَرُوْنَ الْاٰخِرَةَ ﴿٢١﴾

22. Na hamuijali Akhera.

وُجُوْهٌ يَّوْمَئِذٍ نَّاضِرَةٌ ﴿٢٢﴾

23. Nyuso Siku hiyo zitang'aa.

اِلٰى رَبِّهَا نَاظِرَةٌ ﴿٢٣﴾

24. Zikitazama kwa Mola wao.

وَوُجُوْهٌ يَّوْمَئِذٍۭ بَاسِرَةٌ ﴿٢٤﴾

25. Na nyuso (zingine) Siku hiyo zitakunjamana,

تَظُنُّ اَنْ يُّفْعَلَ بِهَا فَاقِرَةٌ ﴿٢٥﴾

26. Zitajua ya kuwa zitafikiwa na msiba uvunjao uti wa mgongo.

كَلَّاۤ اِذَا بَلَغَتِ التَّرَاقِيَ ﴿٢٦﴾

27. Sivyo! (Roho) itakapofikia mitulinga,

وَقِيْلَ مَنْ ۜ رَاقٍ ﴿٢٧﴾

28. Na itasemwa: Ni nani mlozi?

وَّظَنَّ اَنَّهُ الْفِرَاقُ ﴿٢٨﴾

29. Na atajua hakika hii ni (saa ya) kutengana,

وَالْتَفَّتِ السَّاقُ بِالسَّاقِ ﴿٢٩﴾

30. Na utakapoambatanishwa muundi kwa muundi;

اِلٰى رَبِّكَ يَوْمَئِذِ ِۨالْمَسَاقُ ﴿٣٠﴾ ع ١٧

31. Siku hiyo ni kufukuziwa kwa Mola wako.

FUNGU 2

فَلَا صَدَّقَ وَلَا صَلّٰى ﴿٣١﴾

32. Basi hakusadikisha wala hakusali.

وَلٰكِنْ كَذَّبَ وَتَوَلّٰى ﴿٣٢﴾

33. Bali alikadhibisha na akarudi nyuma.

ثُمَّ ذَهَبَ اِلٰۤى اَهْلِهٖ يَتَمَطّٰى ﴿٣٣﴾

34. Kisha alikwenda kwa ahali zake akiringa.

اَوْلٰى لَكَ فَاَوْلٰى ﴿٣٤﴾

35. Maangamizo kwako juu ya maangamizo!

ثُمَّ اَوْلٰى لَكَ فَاَوْلٰى ﴿٣٥﴾

36. Kisha maangamizo kwako juu ya maangamizo!!

اَيَحْسَبُ الْاِنْسَانُ اَنْ يُّتْرَكَ سُدًى ﴿٣٦﴾

37. Je mtu anafikiri kuwa ataachwa bure?

اَلَمْ يَكُ نُطْفَةً مِّنْ مَّنِيٍّ يُّمْنٰى ﴿٣٧﴾

38. Je, hakuwa tone la manii lililotonwa?

ثُمَّ كَانَ عَلَقَةً فَخَلَقَ فَسَوّٰى ﴿٣٨﴾

39. Kisha akawa kidonge cha damu, kisha Akamwumba na Akamsawazisha,

فَجَعَلَ مِنْهُ الزَّوْجَيْنِ الذَّكَرَ وَالْاُنْثٰى ﴿٣٩﴾

40. Kisha Akamfanya namna mbili, kiume na kike.

اَلَيْسَ ذٰلِكَ بِقٰدِرٍ عَلٰۤى اَنْ يُّحْيِۦَ الْمَوْتٰى ﴿٤٠﴾ ع ١٨

41. Je! Huyo Hana uwezo wa kuhuisha wafu?

سُوْرَةُ الدَّهْرِ مَكِّيَّةٌ وَّ هِيَ مَعَ الْبَسْمَلَةِ اثْنَتَانِ وَ ثَلَا ثُوْنَ اٰيَةً وَّ رُكُوْعَانِ

76. SURA AD-DAHR

Imeteremshwa Makka

Ina mafungu 2 na Aya 32 pamoja ana Bismillahi

بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ ①

1. Kwa jina la Allah, Mwingi wa rehema, Mwingi wa ukarimu.

هَلْ اَتٰى عَلَى الْاِنْسَانِ حِيْنٌ مِّنَ الدَّهْرِ لَمْ يَكُنْ شَيْـًٔا مَّذْكُوْرًا ②

2. Je katika zama kuliwahi kutokea muda wowote kwa mwanadamu ambapo hakuwa kitu chenye kustahili kutajwa?

اِنَّا خَلَقْنَا الْاِنْسَانَ مِنْ نُّطْفَةٍ اَمْشَاجٍ ۖ نَّبْتَلِيْهِ فَجَعَلْنٰهُ سَمِيْعًا بَصِيْرًا ③

3. Kwa hakika Tulimwumba mtu kwa tone la manii lililochanganyika ambalo Tunalifanya lipitie katika maumbile mbalimbali; hivyo Tukamfanya asikiaye, aonaye.

اِنَّا هَدَيْنٰهُ السَّبِيْلَ اِمَّا شَاكِرًا وَّ اِمَّا كَفُوْرًا ④

4. Hakika Sisi Tukamwongoza njia awe mwenye shukrani au awe mwenye kukufuru.

اِنَّآ اَعْتَدْنَا لِلْكٰفِرِيْنَ سَلٰسِلَا۠ وَاَغْلٰلًا وَّسَعِيْرًا ⑤

5. Hakika Sisi Tumewaandalia makafiri minyororo na mapingu na Moto uwakao.

اِنَّ الْاَبْرَارَ يَشْرَبُوْنَ مِنْ كَاْسٍ كَانَ مِزَاجُهَا كَافُوْرًا ⑥

6. Hakika watawa watakunywa katika kikombe kilichochanganyika na kafuri.

عَيْنًا يَّشْرَبُ بِهَا عِبَادُ اللّٰهِ يُفَجِّرُوْنَهَا تَفْجِيْرًا ⑦

7. (Itakuwako) chemchem watakayoinywa watumishi wa Allah: wataitiririsha mtiririsho (mzuri).

Sura hii inaitwa *Ad-Dahr* (wakati) na pia inaitwa *Al-Insaan* (Mtu), nayo inaendeleza habari za sura iliyopita na inaeleza juu ya mtu kufikia ukamilifu ambao ndilo kusudi la kuumbwa kwake.

Aya 5. Kafiri hujishughulisha sana na mambo ya dunia na kuiangukia kabisa wala hatumii maungo yake katika kumtumikia Mungu Mwenyezi, kana kwamba anatiwa mnyororo na pingu. Mfano wa hali yake hiyo hiyo ataupewa siku ya Malipo naye atajiona mahabusu. Tamaa ya mwili iletayo mwako moyoni itageuka kuwa moto uwakao sana.

يُوْفُوْنَ بِالنَّذْرِ وَيَخَافُوْنَ يَوْمًا كَانَ شَرُّهٗ مُسْتَطِيْرًا ۝٨

8. Wanazitimiza nadhiri na wanaiogopa Siku ambayo shari yake itaenea sana.

وَيُطْعِمُوْنَ الطَّعَامَ عَلٰى حُبِّهٖ مِسْكِيْنًا وَّيَتِيْمًا وَّاَسِيْرًا ۝٩

9. Na huwalisha chakula maskini na yatima na mfungwa kwa mapenzi Yake.

اِنَّمَا نُطْعِمُكُمْ لِوَجْهِ اللّٰهِ لَا نُرِيْدُ مِنْكُمْ جَزَآءً وَّلَا شُكُوْرًا ۝١٠

10. (Husema): Tunawalisheni kwa ajili ya radhi ya Allah tu, hatutaki kwenu malipo wala shukurani.

اِنَّا نَخَافُ مِنْ رَّبِّنَا يَوْمًا عَبُوْسًا قَمْطَرِيْرًا ۝١١

11. Hakika sisi tunaogopa kutoka kwa Mola wetu Siku yenye shida na taabu.

فَوَقٰىهُمُ اللّٰهُ شَرَّ ذٰلِكَ الْيَوْمِ وَلَقّٰىهُمْ نَضْرَةً وَّسُرُوْرًا ۝١٢

12. Basi Allah Atawalinda katika shari ya Siku hiyo na kuwakutanisha na uchangamfu na furaha.

وَجَزٰىهُمْ بِمَا صَبَرُوْا جَنَّةً وَّحَرِيْرًا ۝١٣

13. Na Atawajazi Bustani na hariri, kwa sababu walisubiri.

مُّتَّكِـِٕيْنَ فِيْهَا عَلَى الْاَرَآئِكِ ۚ لَا يَرَوْنَ فِيْهَا شَمْسًا وَّلَا زَمْهَرِيْرًا ۝١٤

14. Humo wataegemea juu ya viti vya heshima, hawataona humo jua kali wala baridi kali.

وَدَانِيَةً عَلَيْهِمْ ظِلٰلُهَا وَذُلِّلَتْ قُطُوْفُهَا تَذْلِيْلًا ۝١٥

15. Na vivuli vyake vitafikia karibu yao, na matunda yataning'inia chini-chini.

وَيُطَافُ عَلَيْهِمْ بِاٰنِيَةٍ مِّنْ فِضَّةٍ وَّاَكْوَابٍ كَانَتْ قَوَارِيْرَا ۝١٦

16. Na watatembezewa vyombo vya fedha na vikombe vitakavyokuwa vya kioo,

قَوَارِيْرَا مِنْ فِضَّةٍ قَدَّرُوْهَا تَقْدِيْرًا ۝١٧

17. Kioo cha fedha ambacho wamekitengeneza kwa umahiri mkubwa.

وَيُسْقَوْنَ فِيْهَا كَاْسًا كَانَ مِزَاجُهَا زَنْجَبِيْلًا ۝١٨

18. Na humo watanyweshwa kwa kikombe chenye tangawizi.

Aya 9. *'Alaa hubbihii,* "kwa mapenzi yake." au juu ya mapenzi yake" mradi wake ni namna mbili: (1) juu ya kukipenda chakula wao wanakitoa, na (2) wanatoa chakula kuwapa maskini kwa sababu ya kumpenda Mungu. Angalieni jinsi dini ya Kiislamu inavyohimiza wenye mali na wenye uwezo kuwasaidia maskini na inataka kuwa walio chini nao wainuke.

Aya 18. *Kikombe kilichochanganyika na tangawizi.* Neno la *zanjabiil* limetengenezwa

عَيْنًا فِيْهَا تُسَمّٰى سَلْسَبِيْلًا ﴿١٨﴾

19. Humo mna chemchem inayoitwa Salsabil.

وَيَطُوْفُ عَلَيْهِمْ وِلْدَانٌ مُّخَلَّدُوْنَ ۚ
اِذَا رَاَيْتَهُمْ حَسِبْتَهُمْ لُؤْلُؤًا مَّنْثُوْرًا ﴿١٩﴾

20. Na watawazunguka wavulana wasiochakaa, utakapowaona utawadhani kuwa ni lulu zilizotawanywa.

وَ اِذَا رَاَيْتَ ثَمَّ رَاَيْتَ نَعِيْمًا
وَّ مُلْكًا كَبِيْرًا ﴿٢٠﴾

21. Na utakapopatazama utaiona neema na ufalme mkuu.

عٰلِيَهُمْ ثِيَابُ سُنْدُسٍ خُضْرٌ
وَّ اِسْتَبْرَقٌ ۫ وَّحُلُّوْٓا اَسَاوِرَ مِنْ
فِضَّةٍ ۚ وَسَقٰىهُمْ رَبُّهُمْ شَرَابًا طَهُوْرًا ﴿٢١﴾

22. Juu yao (watavaa) nguo za hariri laini ya kijani kibichi na za hariri ya zari, na watavikwa kekee za fedha, na Mola wao Atawanywesha kinywaji safi.

اِنَّ هٰذَا كَانَ لَكُمْ جَزَآءً وَّكَانَ سَعْيُكُمْ
مَّشْكُوْرًا ﴿٢٢﴾ ع ١٩

23. Hakika hayo ni malipo yenu, na juhudi yenu imekubaliwa.

FUNGU 2

اِنَّا نَحْنُ نَزَّلْنَا عَلَيْكَ الْقُرْاٰنَ تَنْزِيْلًا ﴿٢٣﴾ ۚ

24. Hakika Sisi Tumekuteremshia Qur'an hatua kwa hatua.

---

kwa maneno mawili: *zana* na *jabal* yaani *kupanda kilima.* Tabia ya tangawizi ni kuleta joto mwilini; hivyo inasemekana kama mtu anakunywa kikombe cha mapenzi ya Allah anakuwa kama aliyekunywa tangawizi, na anapata joto na kwa joto hilo anaweza kupanda vilima vya mashaka na udhia na anaweza kufanya mambo ya kustaajabisha watu.

Aya 19. Mtu ambaye anaziacha tamaa zake na kujiepusha na dhambi zote kwa ajili ya Allah moyo wake hutulia, kana kwamba amenyweshwa kinywaji kilichochanganywa na kafuri (karafuu maiti) ambayo ni kiburudisho, tena inafuta athari ya sumu imwangamizayo mtu.

Tangawizi inamrudishia mtu nguvu yake iliyopotea na humpa uwezo wa kujitahidi sana. Moyo wa mtu ukiisha kutakasika kwa kafuri, atapewa kikombe kingine kitiwacho tangawizi, yaani ataongezewa uwezo wa kutenda wema.

Salsabila maana yake ni uliza njia, yaani mumini akisha kupewa nguvu ya kufanya mema, hatatamani cho chote ila kuishika njia ya Allah tu na kuzidi kumkaribia Yeye.

Daraja tatu za mwendeleo wa mumini - kuepukana na dhambi, kutenda mema na kusogea karibu sana na Mungu - zimefananishwa na kikombe cha kafuri na kikombe cha tangawizi na *salsabila.*

Tofauti ya vikombe na chemchem yaonekana dhahiri. Kilichomo ndani ya kikombe lazima kiishe, na maji ya chemchem hububujika nyakati zote. Maana mumini atapita zile daraja mbili za kwanza, lakini kuonana na Mungu hakuna mwisho. Yeye huwa na maonyesho Yake mapya kila wakati (sura 55:30).

Kuzifananisha neema za kiroho na kinywaji au chakula kunajulisha ya kuwa uzima wa waaminio huko Peponi utategemea kukaa na Mungu tu (sura 9:72).

فَاصْبِرْ لِحُكْمِ رَبِّكَ وَلَا تُطِعْ مِنْهُمْ
اٰثِمًا اَوْ كَفُوْرًا ﴿٢٤﴾

25. Basi ungojee hukumu ya Mola wako wala usimtii miongoni mwao mwenye dhambi au mwenye kukufuru.

وَاذْكُرِ اسْمَ رَبِّكَ بُكْرَةً وَّاَصِيْلًا ﴿٢٥﴾

26. Na likumbuke jina la Mola wako asubuhi na jioni;

وَمِنَ الَّيْلِ فَاسْجُدْ لَهٗ وَسَبِّحْهُ لَيْلًا
طَوِيْلًا ﴿٢٦﴾

27. Na Msujudie Yeye sehemu fulani ya usiku, na umtukuze usiku mzima.

اِنَّ هٰٓؤُلَآءِ يُحِبُّوْنَ الْعَاجِلَةَ وَيَذَرُوْنَ
وَرَآءَهُمْ يَوْمًا ثَقِيْلًا ﴿٢٧﴾

28. Kwa hakika watu hawa huyapenda wayapatayo upesi na huiacha nyuma yao Siku nzito.

نَحْنُ خَلَقْنٰهُمْ وَشَدَدْنَآ اَسْرَهُمْ ۚ
وَاِذَا شِئْنَا بَدَّلْنَآ اَمْثَالَهُمْ تَبْدِيْلًا ﴿٢٨﴾

29. Sisi Tumewaumba na Tukaimarisha viungo vyao, na Tutakapotaka Tutazibadilisha kabisa sura zao.

اِنَّ هٰذِهٖ تَذْكِرَةٌ ۚ فَمَنْ شَآءَ اتَّخَذَ
اِلٰى رَبِّهٖ سَبِيْلًا ﴿٢٩﴾

30. Hakika huu ni ukumbusho basi anayetaka ashike njia kwa Mola wake.

وَمَا تَشَآءُوْنَ اِلَّآ اَنْ يَّشَآءَ اللّٰهُ ؕ اِنَّ اللّٰهَ
كَانَ عَلِيْمًا حَكِيْمًا ﴿٣٠﴾

31. Na hamuwezi kutekeleza tamaa zenu isipokuwa kama Allah Apende. Hakika Allah ni Mwenye kujua, Mwenye hekima.

يُّدْخِلُ مَنْ يَّشَآءُ فِيْ رَحْمَتِهٖ ؕ وَالظّٰلِمِيْنَ
اَعَدَّ لَهُمْ عَذَابًا اَلِيْمًا ﴿٣١﴾ ع

32. Humwingiza Anayemtaka katika rehema Yake, na wadhalimu Amewawekea tayari adhabu iumizayo.

سُوْرَةُ الْمُرْسَلَاتِ مَكِّيَّةٌ وَّ هِيَ مَعَ الْبَسْمَلَةِ اِحْدٰى وَ خَمْسُوْنَ اٰيَةً وَّ رُكُوْعَانِ

77. SURA AL-MURSALAAT

Imeteremshwa Makka

Ina mafungu 2 na Aya 51 pamoja na Bismillahi

بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ ①

1. Kwa jina la Allah, Mwingi wa rehema, Mwingi wa ukarimu.

وَالْمُرْسَلٰتِ عُرْفًا ۙ ②

2. Naapa kwa (pepo) zinazopelekwa kwa uanana,

فَالْعٰصِفٰتِ عَصْفًا ۙ ③

3. Tena kwa zile ziendazo kasi,

وَّالنّٰشِرٰتِ نَشْرًا ۙ ④

4. Na kwa wale wenye kuueneza (ujumbe) kikamilifu.

فَالْفٰرِقٰتِ فَرْقًا ۙ ⑤

5. Na kisha wanazibainisha tofauti kwa uwazi.

فَالْمُلْقِيٰتِ ذِكْرًا ۙ ⑥

6. Na kwa wale wanaopeleka ukumbusho.

عُذْرًا اَوْ نُذْرًا ۙ ⑦

7. Kwa hoja au kwa onyo,

اِنَّمَا تُوْعَدُوْنَ لَوَاقِعٌ ؕ ⑧

8. Kwa hakika yale mnayoahidiwa bila shaka yatatokea.

فَاِذَا النُّجُوْمُ طُمِسَتْ ۙ ⑨

9. Basi nyota zitakapopotezwa (nuru zao).

وَ اِذَا السَّمَآءُ فُرِجَتْ ۙ ⑩

10. Na mbingu zitakapopasuliwa,

وَ اِذَا الْجِبَالُ نُسِفَتْ ۙ ⑪

11. Na milima itakapong'olewa,

وَ اِذَا الرُّسُلُ اُقِّتَتْ ؕ ⑫

12. Na Mitume watakapokusanywa katika wakati maalumu,

لِاَيِّ يَوْمٍ اُجِّلَتْ ؕ ⑬

13. Siku gani imekadiriwa kuwa wakati wao?

Sura hii imepata jina lake katika Aya ya 2, na ilishuka Makka yumkini katika mwaka wa 4 wa Utume.

Aya 8. Ahadi zilizotolewa na Mtume *s.a.w.* ziwe za dunia hii au Akhera lazima zitatimia.

Aya 9. Nyota mradi wake ni masheikh na waalimu wa dini, ambao hawatakuwa na maarifa na nuru ya moyo.

لِيَوْمِ الْفَصْلِ ﴿١٤﴾

14. Kwa ajili ya siku ya Hukumu.

وَمَآ اَدْرٰىكَ مَا يَوْمُ الْفَصْلِ ﴿١٥﴾

15. Na nini kitakujulisha siku ya hukumu ni nini?

وَيْلٌ يَّوْمَئِذٍ لِّلْمُكَذِّبِيْنَ ﴿١٦﴾

16. Ole wao Siku hiyo wanaokadhibisha!

اَلَمْ نُهْلِكِ الْاَوَّلِيْنَ ﴿١٧﴾

17. Je! Hatukuwaangamiza (watu) wa awali?

ثُمَّ نُتْبِعُهُمُ الْاٰخِرِيْنَ ﴿١٨﴾

18. Kisha Tukawaandamizia (watu) wengine.

كَذٰلِكَ نَفْعَلُ بِالْمُجْرِمِيْنَ ﴿١٩﴾

19. Hivi ndivyo Tuwafanyiavyo wakosefu.

وَيْلٌ يَّوْمَئِذٍ لِّلْمُكَذِّبِيْنَ ﴿٢٠﴾

20. Ole wao Siku hiyo wanaokadhibisha!

اَلَمْ نَخْلُقْكُّمْ مِّنْ مَّآءٍ مَّهِيْنٍ ﴿٢١﴾

21. Je! Hatukuwaumbeni kwa maji yaliyo dhalili?

فَجَعَلْنٰهُ فِيْ قَرَارٍ مَّكِيْنٍ ﴿٢٢﴾

22. Kisha Tukayaweka mahali pa utulivu?

اِلٰى قَدَرٍ مَّعْلُوْمٍ ﴿٢٣﴾

23. Mpaka muda maalumu,

فَقَدَرْنَا ۟ فَنِعْمَ الْقٰدِرُوْنَ ﴿٢٤﴾

24. Na Tukakadiria nasi ni Wakadiriao wema walioje!

وَيْلٌ يَّوْمَئِذٍ لِّلْمُكَذِّبِيْنَ ﴿٢٥﴾

25. Ole wao Siku hiyo wanaokadhibisha!

اَلَمْ نَجْعَلِ الْاَرْضَ كِفَاتًا ﴿٢٦﴾

26. Je! Sisi Hatukuifanya ardhi yenye kukusanya.

اَحْيَآءً وَّاَمْوَاتًا ﴿٢٧﴾

27. Wazima na wafu?

وَّجَعَلْنَا فِيْهَا رَوَاسِيَ شٰمِخٰتٍ وَّاَسْقَيْنٰكُمْ مَّآءً فُرَاتًا ﴿٢٨﴾

28. Na ndani yake Tukaweka milima mirefu na Tumewanywesheni maji matamu.

Aya 21. Hapa watu wote wanaambiwa asili yao ni moja, wameumbwa kwa maji yaliyo dhalili: matajiri, maskini, wafalme, raia na watu wote, hivyo kubaguana na kudharauliana hakuna maana.

Aya 26-27. Aya hizi zinaeleza ya kuwa ardhi imepewa nguvu ya uvutano, cho chote lazima kitakaa papa hapa. Ukitupa jiwe juu lazima litarudi chini. Cho chote kiwe kizima au kilichokufa, awe Isa au mtu mwingine, hawezi kuponyoka ndani ya ardhi hii. Makao yao vyote ni hapa hapa ardhini.

وَيْلٌ يَّوْمَئِذٍ لِّلْمُكَذِّبِيْنَ ﴿٢٩﴾

29. Ole wao Siku hiyo wanaokadhibisha!

اِنْطَلِقُوْٓا اِلٰى مَا كُنْتُمْ بِهٖ تُكَذِّبُوْنَ ﴿٣٠﴾ ۚ

30. Nendeni kwenye yale mliyokuwa mkikadhibisha.

اِنْطَلِقُوْٓا اِلٰى ظِلٍّ ذِيْ ثَلٰثِ شُعَبٍ ﴿٣١﴾ ۙ

31. Nendeni kwenye kivuli chenye matawi matatu,

لَّا ظَلِيْلٍ وَّلَا يُغْنِيْ مِنَ اللَّهَبِ ﴿٣٢﴾ ؕ

32. Hayatoi kivuli wala hayafai kwa Moto uwakao.

اِنَّهَا تَرْمِيْ بِشَرَرٍ كَالْقَصْرِ ﴿٣٣﴾ ۚ

33. Hakika huo hutoa cheche zilizo kama ngome.

كَاَنَّهٗ جِمٰلَتٌ صُفْرٌ ﴿٣٤﴾ ؕ

34. Kana kwamba ni ngamia wa rangi ya njano.

وَيْلٌ يَّوْمَئِذٍ لِّلْمُكَذِّبِيْنَ ﴿٣٥﴾

35. Ole wao Siku hiyo wanaokadhibisha!

هٰذَا يَوْمُ لَا يَنْطِقُوْنَ ﴿٣٦﴾ ۙ

36. Hii ni Siku ambayo hawatazungumza.

وَلَا يُؤْذَنُ لَهُمْ فَيَعْتَذِرُوْنَ ﴿٣٧﴾

37. Wala hawatapewa ruhusa kutoa udhuru.

وَيْلٌ يَّوْمَئِذٍ لِّلْمُكَذِّبِيْنَ ﴿٣٨﴾

38. Ole wao Siku hiyo wanaokadhibisha!

هٰذَا يَوْمُ الْفَصْلِ ۚ جَمَعْنٰكُمْ وَالْاَوَّلِيْنَ ﴿٣٩﴾

39. Hii ni Siku ya Hukumu: Tumewakusanyeni ninyi na waliotangulia.

فَاِنْ كَانَ لَكُمْ كَيْدٌ فَكِيْدُوْنِ ﴿٤٠﴾

40. Basi ikiwa mnayo hila ifanyeni juu Yangu.

وَيْلٌ يَّوْمَئِذٍ لِّلْمُكَذِّبِيْنَ ﴿٤١﴾ ع

41. Ole wao Siku hiyo wanaokadhibisha!

FUNGU 2

اِنَّ الْمُتَّقِيْنَ فِيْ ظِلٰلٍ وَّعُيُوْنٍ ﴿٤٢﴾ ۙ

42. Bila shaka wamchao Mungu watakuwa ndani ya (bustani zenye) vivuli na chemchem,

وَّفَوَاكِهَ مِمَّا يَشْتَهُوْنَ ﴿٤٣﴾ ؕ

43. Na matunda wanayoyapenda.

Aya 31-32. Wakristo wanadhani kuwa utatu, yaani Mungu Baba, Mungu Mwana na Mungu Roho Mtakatifu utawaokoa. Hapa wanaambiwa kivuli chao hiki chenye matawi matatu hakitawafaa kwa Moto uwakao.

كُلُوْا وَاشْرَبُوْا هَنِيْٓـًٔا بِمَا كُنْتُمْ تَعْمَلُوْنَ ﴿٤٣﴾

44. Kuleni na kunyweni kwa furaha kwa sababu ya yale mliyokuwa mkitenda.

اِنَّا كَذٰلِكَ نَجْزِى الْمُحْسِنِيْنَ ﴿٤٤﴾

45. Hakika Sisi ndivyo hivi Tunavyo-walipa watendao mema.

وَيْلٌ يَّوْمَئِذٍ لِّلْمُكَذِّبِيْنَ ﴿٤٥﴾

46. Ole wao Siku hiyo wanaokadhibisha!

كُلُوْا وَتَمَتَّعُوْا قَلِيْلًا اِنَّكُمْ مُّجْرِمُوْنَ ﴿٤٦﴾

47. Kuleni na mjifurahishe kidogo, hakika ninyi ni wakosefu.

وَيْلٌ يَّوْمَئِذٍ لِّلْمُكَذِّبِيْنَ ﴿٤٧﴾

48. Ole wao Siku hiyo wanaokadhibisha!

وَاِذَا قِيْلَ لَهُمُ ارْكَعُوْا لَا يَرْكَعُوْنَ ﴿٤٨﴾

49. Na walipokuwa wakiambiwa: Inameni, hawainami.

وَيْلٌ يَّوْمَئِذٍ لِّلْمُكَذِّبِيْنَ ﴿٤٩﴾

50. Ole wao Siku hiyo wanaokadhibisha!

فَبِاَيِّ حَدِيْثٍ بَعْدَهٗ يُؤْمِنُوْنَ ﴿٥٠﴾ ع ٢ ٣٣

51. Basi hadithi gani baada ya hii wataiamini?

سُوْرَةُ النَّبَاِ مَكِّيَّةٌ وَّ هِیَ مَعَ الْبَسْمَلَةِ اِحْدٰی وَ اَرْبَعُوْنَ اٰیَةً وَّ رُكُوْعَانِ

78. SURA AN-NABA'

Imeteremshwa Makka

Ina mafungu 2 na Aya 41 pamoja na Bismillahi

JUZU 30

بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ ①

1. Kwa jina la Allah, Mwingi wa rehema, Mwingi wa ukarimu.

عَمَّ يَتَسَآءَلُوْنَ ②

2. Habari gani wanaulizana?

عَنِ النَّبَاِ الْعَظِيْمِ ③

3. Kuhusu habari iliyo kuu.

الَّذِیْ هُمْ فِيْهِ مُخْتَلِفُوْنَ ④

4. Ni (habari) hiyo hiyo wanayohitilafiana wao kwa wao?

كَلَّا سَيَعْلَمُوْنَ ⑤

5. Siyo! Hivi karibuni watajua.

ثُمَّ كَلَّا سَيَعْلَمُوْنَ ⑥

6. Tena siyo! Hivi karibuni watajua.

اَلَمْ نَجْعَلِ الْاَرْضَ مِهٰدًا ⑦

7. Je! Hatukuifanya ardhi kuwa tandiko?

وَّالْجِبَالَ اَوْتَادًا ⑧

8. Na milima kuwa misumari?

وَّخَلَقْنٰكُمْ اَزْوَاجًا ⑨

9. Na Tukawaumbeni jozi-jozi;

وَّجَعَلْنَا نَوْمَكُمْ سُبَاتًا ⑩

10. Na Tukaufanya usingizi wenu mapumziko;

وَّجَعَلْنَا الَّيْلَ لِبَاسًا ⑪

11. Na Tukaufanya usiku kivazi;

وَّجَعَلْنَا النَّهَارَ مَعَاشًا ⑫

12. Na Tukaufanya mchana kwa ajili ya kutafutia riziki;

Inasemekana ya kuwa sura hii ni ya siku za mwanzo Mtume alipokuwa Makka. Inaitwa *An-Naba'* maana zimetajwa ndani yake habari zilizo kuu: habari za ushindi wa Uislamu, au habari za Qur'an au habari za kufufuka baada ya kufa, moja ya hizi au zote tatu.

Aya 3. *Habari iliyo kuu* ni habari ya Kiyama. Kadhalika Qur'an na Mtume *s.a.w.* ni habari zilizo kuu ambazo walikuwa wakihitalafiana.

Aya 6. *Hivi karibuni watajua,* yaani watajua ukweli wa Qur'an, wa Mtume *s.a.w.* na wa Kiyama.

13. Na Tukajenga juu yenu (mbingu) saba madhubuti;

وَّبَنَيْنَا فَوْقَكُمْ سَبْعًا شِدَادًا ﴿١٣﴾

14. Na Tukaifanya taa ing'aayo sana;

وَّجَعَلْنَا سِرَاجًا وَّهَّاجًا ﴿١٤﴾

15. Na Tukateremsha maji yaangukayo kwa kasi kutoka mawinguni.

وَّاَنْزَلْنَا مِنَ الْمُعْصِرٰتِ مَآءً ثَجَّاجًا ﴿١٥﴾

16. Ili kwayo Tuoteshe mbegu na mimea,

لِّنُخْرِجَ بِهٖ حَبًّا وَّنَبَاتًا ﴿١٦﴾

17. Na mabustani yenye miti iliyosongana.

وَّجَنّٰتٍ اَلْفَافًا ﴿١٧﴾

18. Kwa hakika siku ya Hukumu ni wakati uliokadiriwa.

اِنَّ يَوْمَ الْفَصْلِ كَانَ مِيْقَاتًا ﴿١٨﴾

19. Siku itakapopigwa parapanda nanyi mtafika makundi-makundi;

يَّوْمَ يُنْفَخُ فِي الصُّوْرِ فَتَاْتُوْنَ اَفْوَاجًا ﴿١٩﴾

20. Na mbingu zitafunguliwa ndipo zitakuwa zenye milango mingi;

وَّفُتِحَتِ السَّمَآءُ فَكَانَتْ اَبْوَابًا ﴿٢٠﴾

21. Na milima itatembezwa na kuelekea mabondeni.

وَّسُيِّرَتِ الْجِبَالُ فَكَانَتْ سَرَابًا ﴿٢١﴾

22. Kwa hakika Jahanamu inavizia,

اِنَّ جَهَنَّمَ كَانَتْ مِرْصَادًا ﴿٢٢﴾

23. Ni makazi ya waasi,

لِّلطّٰغِيْنَ مَاٰبًا ﴿٢٣﴾

24. Wakikaa humo karne nyingi,

لّٰبِثِيْنَ فِيْهَآ اَحْقَابًا ﴿٢٤﴾

25. Hawataonja humo kitu cha baridi wala kinywaji chochote,

لَا يَذُوْقُوْنَ فِيْهَا بَرْدًا وَّلَا شَرَابًا ﴿٢٥﴾

Aya 24. *Karne nyingi.* Adhabu ya Jahanamu itakuwa kwa muda mrefu. Makafiri na watenda mabaya wakiisha kupokea adhabu kadiri ya uovu waliotenda watatolewa nje na kupelekwa Peponi. Moto si makao ya milele ya wanadamu ambao waliumbwa kwa ajili ya kumwabudu Mungu. Wenye kumtii Mola wao watafika Kwake moja kwa moja, na waasi watazuiliwa njiani wapate kulipishwa maovu yao na kuhuishwa ile sura ya kiroho waliyoiharibu. Jinsi mtoto hupata umbo zuri tumboni mwa mama yake limfaalo kukaa hapa duniani, ndivyo mwenye dhambi atakavyopewa mle ndani ya Jahanamu umbo kamilifu limwezeshalo kukaa huko Peponi. Kwa ajili hii Moto umeitwa kuwa mamaye mwenye dhambi (sura 101:10). Akiisha kutakasika hivyo atamlaki Allah.

Mungu si mdhalimu awalipe wakosefu adhabu isiyokwisha kwa sababu ya yale matendo waliyoyatenda katika maisha yao mafupi. Amesema Mwenyewe, "Rehema yangu hukienea kila kitu" (sura 7:157). Basi adhabu ya Moto iwe kali namna gani, itakoma. Lakini kule Peponi

اِلَّا حَمِيْمًا وَّغَسَّاقًا ﴿٢٥﴾

26. Ila maji yachemkayo sana na usaha wenye kunuka.

جَزَآءً وِّفَاقًا ﴿٢٦﴾

27. Malipo muafaka.

اِنَّهُمْ كَانُوْا لَا يَرْجُوْنَ حِسَابًا ﴿٢٧﴾

28. Wao hawakutegemea asilan kuwepo na hesabu yoyote.

وَّكَذَّبُوْا بِاٰيٰتِنَا كِذَّابًا ﴿٢٨﴾

29. Nao walizikadhibisha sana Aya Zetu.

وَكُلَّ شَيْءٍ اَحْصَيْنٰهُ كِتٰبًا ﴿٢٩﴾

30. Na kila kitu Tumekihesabu Kitabuni.

فَذُوْقُوْا فَلَنْ نَّزِيْدَكُمْ اِلَّا عَذَابًا ﴿٣٠﴾ ع

31. Basi onjeni! Nasi Hatutawazidishieni (kitu) ila adhabu.

FUNGU 2

اِنَّ لِلْمُتَّقِيْنَ مَفَازًا ﴿٣١﴾

32. Bila shaka wamchao Allah (wamekadiriwa kupata) mafanikio makubwa sana:

حَدَآئِقَ وَاَعْنَابًا ﴿٣٢﴾

33. Mabustani na mizabibu,

وَّكَوَاعِبَ اَتْرَابًا ﴿٣٣﴾

34. Na mabikira wanaolingana umri,

وَّكَاْسًا دِهَاقًا ﴿٣٤﴾

35. Na vikombe vilivyojaa;

لَا يَسْمَعُوْنَ فِيْهَا لَغْوًا وَّلَا كِذّٰبًا ﴿٣٥﴾ ج

36. Hawatasikia humo maneno ya upuuzi wala uongo hata kidogo;

جَزَآءً مِّنْ رَّبِّكَ عَطَآءً حِسَابًا ﴿٣٦﴾

37. Ni malipo toka kwa Mola wako zawadi iliyo kamilika

رَّبِّ السَّمٰوٰتِ وَالْاَرْضِ وَمَا بَيْنَهُمَا الرَّحْمٰنِ لَا يَمْلِكُوْنَ مِنْهُ خِطَابًا ﴿٣٧﴾ ج

38. Mwumba wa mbingu na ardhi na vilivyomo kati yao, ni Rahmani; hawatakuwa na haki ya kumwambia neno.

يَوْمَ يَقُوْمُ الرُّوْحُ وَالْمَلٰٓئِكَةُ صَفًّا ۙ لَّا يَتَكَلَّمُوْنَ اِلَّا مَنْ اَذِنَ لَهُ الرَّحْمٰنُ وَقَالَ صَوَابًا ﴿٣٨﴾

39. Siku ambayo atasimama Roho na Malaika safu-safu; hawatazungumza ila ambaye Rahmani Amemwidhinisha na atasema yaliyo sawa.

kuliko raha na starehe Allah atawajazi waaminio wema wao na kuwaongezea bakhshishi vile vile kwa hisani Yake. Na zawadi yake Allah haina kikomo (sura 11:109).

ذٰلِكَ الْيَوْمُ الْحَقُّ ۚ فَمَنْ شَآءَ اتَّخَذَ اِلٰى رَبِّهٖ مَاٰبًا ﴿٣٩﴾

40. Hiyo ndiyo Siku ya haki, basi anayetaka ashike makao kwa Mola wake.

اِنَّآ اَنْذَرْنٰكُمْ عَذَابًا قَرِيْبًا ۚ يَّوْمَ يَنْظُرُ الْمَرْءُ مَا قَدَّمَتْ يَدٰهُ وَيَقُوْلُ الْكٰفِرُ يٰلَيْتَنِىْ كُنْتُ تُرٰبًا ﴿٤٠﴾ ع

41. Hakika Tumewatahadharisheni na adhabu iliyo karibu: Siku ambayo mtu atayaona iliyoyatanguliza mikono yake miwili, na kafiri atasema: Laiti ningalikuwa udongo.

Aya 41. *Adhabu iliyo karibu,* yaani adhabu ya kushindwa kwa makafiri iliyotokea katika vita vya Badri, na pia kushindwa Makka. Allah anasema, aliwatahadharisha kwa adhabu hizo ili wakae hali ya kujua kwamba kama vile zilivyotokea hizo na ya Kiyama pia itatokea.

سُوْرَةُ النَّازِعَاتِ مَكِّيَّةٌ وَّ هِيَ مَعَ الْبَسْمَلَةِ سَبْعٌ وَّ اَرْبَعُوْنَ اٰيَةً وَّ رُكُوْعَانِ

79. SURA AN-NAAZI'AAT

Imeteremshwa Makka

Ina mafungu 2 na Aya 47 pamoja na Bismillahi

بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ ۝

1. Kwa jina la Allah, Mwingi wa rehema, Mwingi wa ukarimu.

وَالنّٰزِعٰتِ غَرْقًا ۝١

2. Naapa kwa wale waendao chini ya maji na kuvuta, (au) wavutao kwa madhumuni ya kuzamisha,

وَّالنّٰشِطٰتِ نَشْطًا ۝٢

3. Na kwa wale wenye kusherehekea sana,

وَّالسّٰبِحٰتِ سَبْحًا ۝٣

4. Na kwa wale wenye kuogelea sana,

فَالسّٰبِقٰتِ سَبْقًا ۝٤

5. Na kwa wale washindanao wao kwa wao,

فَالْمُدَبِّرٰتِ اَمْرًا ۝٥

6. Na kwa wale wafanyao mipango ya kazi fulani muhimu,

يَوْمَ تَرْجُفُ الرَّاجِفَةُ ۝٦

7. Siku ambayo wenye kutetemeka watatetemeka mno,

تَتْبَعُهَا الرَّادِفَةُ ۝٧

8. (Na) kitafuata nyuma yake kiandamiacho.

قُلُوْبٌ يَّوْمَئِذٍ وَّاجِفَةٌ ۝٨

9. Siku hiyo mioyo itapiga sana.

اَبْصَارُهَا خَاشِعَةٌ ۝٩

10. Macho yao yatatazama chini.

Kwa kauli ya Abdullah bin Abbas na Abdullah bin Zubair, sura hii ilishuka Makka na wafasiri wote wanakubaliana juu ya jambo hili. Jina la sura hii linatoka katika Aya ya 2.

Aya 2-6. Aya hizi, pamoja na mambo mengine, pia zimeeleza mambo ambayo mtu akiyashika atafanikiwa: (1) *wavutao kwa madhumuni ya kuzamisha,* yaani mtu aivute nafsi yake kwa nguvu mbali na matamanio mabaya: kisha aigharikishe katika mambo mema; (2) *wenye kusherehekea sana,* yaani mtu aone furaha na uzuri katika juhudi hiyo, maana kama hakuifurahia hawezi kuendelea nayo; (3) *waogeleao sana,* yaani, baada ya mambo hayo mawili, jambo la tatu litakuwa kuona wepesi katika juhudi hiyo na kuizoea; (4) *Washindanao wao kwa wao,* yaani mtu asiridhike na hali njema aliyofikia bali afanye bidii kupita mbele na kuzidi katika wema; (5) *wafanyao mipango ya kazi fulani muhimu,* yaani, siyo kwamba mtu atosheke na hali yake mwenyewe tu, bali pia afanye bidii mambo yaongoke na wengine waingie katika juhudi kama yake.

يَقُوْلُوْنَ ءَاِنَّا لَمَرْدُوْدُوْنَ فِى الْحَافِرَةِ ﴿١١﴾

11. (Watu hao) watasema: Je! kweli tutarudishwa katika hali ya kwanza?

ءَاِذَا كُنَّا عِظَامًا نَّخِرَةً ﴿١٢﴾

12. Hata tukiwa tumeshakuwa mifupa mibovu?

قَالُوْا تِلْكَ اِذًا كَرَّةٌ خَاسِرَةٌ ﴿١٣﴾

13. Hapo watasema: Basi marudio haya ni yenye hasara.

فَاِنَّمَا هِىَ زَجْرَةٌ وَّاحِدَةٌ ﴿١٤﴾

14. (Sikilizeni) Kwa hakika hiyo itakuwa tu ni (sauti ya) karipio kubwa.

فَاِذَا هُمْ بِالسَّاهِرَةِ ﴿١٥﴾

15. Mara watakuwa uwanjani!

هَلْ اَتٰىكَ حَدِيْثُ مُوْسٰى ﴿١٦﴾

16. Je! imekufikia hadithi ya Musa?

اِذْ نَادٰىهُ رَبُّهٗ بِالْوَادِ الْمُقَدَّسِ طُوًى ﴿١٧﴾

17. Mola wake Alipomwita katika bonde takatifu (liitwalo) Tuwaa,

اِذْهَبْ اِلٰى فِرْعَوْنَ اِنَّهٗ طَغٰى ﴿١٨﴾

18. (Akinena): Nenda kwa Firauni, hakika yeye amezidi kuasi.

فَقُلْ هَلْ لَّكَ اِلٰٓى اَنْ تَزَكّٰى ﴿١٩﴾

19. Kisha muulize: Je yawezekana kwako kujitakasa?

وَاَهْدِيَكَ اِلٰى رَبِّكَ فَتَخْشٰى ﴿٢٠﴾

20. Nami nikuongoze kwa Mola wako ili umche.

فَاَرٰىهُ الْاٰيَةَ الْكُبْرٰى ﴿٢١﴾

21. Basi alimwonyesha Ishara kubwa.

فَكَذَّبَ وَعَصٰى ﴿٢٢﴾

22. Lakini alikadhibisha na akaasi.

ثُمَّ اَدْبَرَ يَسْعٰى ﴿٢٣﴾

23. Kisha alirudi nyuma kwa pupa.

فَحَشَرَ فَنَادٰى ﴿٢٤﴾

24. Kisha aliwakusanya (watu) akanadi.

فَقَالَ اَنَا رَبُّكُمُ الْاَعْلٰى ﴿٢٥﴾

25. Akasema: Mimi ndiye mola wenu mkuu.

فَاَخَذَهُ اللّٰهُ نَكَالَ الْاٰخِرَةِ وَالْاُوْلٰى ﴿٢٦﴾

26. Hapo Allah Akamkamata kwa adhabu ya Akhera na ya dunia.

اِنَّ فِىْ ذٰلِكَ لَعِبْرَةً لِّمَنْ يَّخْشٰى ﴿٢٧﴾

27. Kwa hakika katika hayo limo onyo kwa yule aogopaye.

FUNGU 2

ءَاَنْتُمْ اَشَدُّ خَلْقًا اَمِ السَّمَآءُ ؕ بَنٰىهَا ﴿٢٨﴾

28. Je, ninyi ni wenye umbo gumu zaidi au mbingu aliyoiumba?

رَفَعَ سَمْكَهَا فَسَوّٰىهَا ﴿٢٩﴾

29. Akaiinua kimo chake na Akaitengeneza vizuri,

وَاَغْطَشَ لَيْلَهَا وَاَخْرَجَ ضُحٰىهَا ﴿٣٠﴾

30. Na Akaufunika usiku wake, na Akaitokeza asubuhi yake;

وَالْاَرْضَ بَعْدَ ذٰلِكَ دَحٰىهَا ﴿٣١﴾

31. Na ardhi baada ya hayo Akaisawazisha.

اَخْرَجَ مِنْهَا مَآءَهَا وَمَرْعٰىهَا ﴿٣٢﴾

32. Na Akatoa ndani yake maji yake na malisho yake;

وَالْجِبَالَ اَرْسٰىهَا ﴿٣٣﴾

33. Na milima Akaiimarisha:

مَتَاعًا لَّكُمْ وَلِاَنْعَامِكُمْ ﴿٣٤﴾

34. Kuwafaidieni ninyi na wanyama wenu.

فَاِذَا جَآءَتِ الطَّآمَّةُ الْكُبْرٰى ﴿٣٥﴾

35. Basi utakapofika ule msiba mkubwa kabisa,

يَوْمَ يَتَذَكَّرُ الْاِنْسَانُ مَا سَعٰى ﴿٣٦﴾

36. Siku ambayo mtu atakumbuka aliyoyafanyia bidii,

وَبُرِّزَتِ الْجَحِيْمُ لِمَنْ يَّرٰى ﴿٣٧﴾

37. Na moto mkali utaonyeshwa kwa yule aonaye.

فَاَمَّا مَنْ طَغٰى ﴿٣٨﴾

38. Ama kwa yule aliyeasi kupita kiasi,

وَاٰثَرَ الْحَيٰوةَ الدُّنْيَا ﴿٣٩﴾

39. Na akapendelea zaidi maisha ya dunia,

فَاِنَّ الْجَحِيْمَ هِىَ الْمَاْوٰى ﴿٤٠﴾

40. Basi kwa hakika Jahanamu ndiyo makao.

وَاَمَّا مَنْ خَافَ مَقَامَ رَبِّهٖ وَنَهَى النَّفْسَ عَنِ الْهَوٰى ﴿٤١﴾

41. Na ama yule aliyeyaogopa makamu ya Mola wake, na akaikataza nafsi matamanio maovu,

Aya 41. Mtu ajizuiaye kuyafuata matamanio ya nafsi yake, ataingia Peponi. Ndiyo maana ya kusema amwogopaye Mola wake huwa na mabustani mawili - moja hapa duniani na la pili katika Akhera (sura 55:47). Bustani la hapa duniani linafanana na mbegu tu iliyopandwa shambani ikafichika ndani ya udongo. Katika Akhera nuru watakayopewa waaminio itaonekana waziwazi, hata makafiri watatamani kujichukulia sehemu ya mwanga wake. Lakini watanyimwa kwa kuwa hawakuwa nao duniani (sura 57:14). Adhabu ya Jahanamu vilevile inaanza katika dunia hii. Lakini pengine mpotevu hauoni upotevu wake. Siku ya Kiyama atautambua barabara (sura 17:73; 20:129; 22:47; 43:41; 10:44; 27:83; 41:18; 2:11; 3:8). Mpotevu ambaye

فَاِنَّ الْجَنَّةَ هِیَ الْمَاْوٰی ﴿۴۱﴾

42. Basi kwa hakika Pepo ndiyo makao.

یَسْـَٔلُوْنَكَ عَنِ السَّاعَةِ اَیَّانَ مُرْسٰىهَا ﴿۴۲﴾

43. Wanakuuliza juu ya saa ile kutokea kwake kutakuwa lini.

فِیْمَ اَنْتَ مِنْ ذِكْرٰىهَا ﴿۴۳﴾

44. Unafikiria nini kuitaja?

اِلٰی رَبِّكَ مُنْتَهٰىهَا ﴿۴۴﴾

45. Mwisho wake ni kwa Mola wako.

اِنَّمَاۤ اَنْتَ مُنْذِرُ مَنْ یَّخْشٰىهَا ﴿۴۵﴾

46. Wewe ni Mwonyaji tu kwa yule anayeiogopa.

كَاَنَّهُمْ یَوْمَ یَرَوْنَهَا لَمْ یَلْبَثُوْۤا اِلَّا عَشِیَّةً اَوْ ضُحٰىهَا ﴿۴۶﴾

47. Siku watakapoiona watakuwa kana kwamba hawakukaa ila kwa jioni moja au asubuhi yake.

سُوْرَةُ عَبَسَ مَكِّيَّةٌ وَّ هِيَ مَعَ الْبَسْمَلَةِ ثَلَاثٌ وَّ اَرْبَعُوْنَ اٰيَةً وَّ رُكُوْعٌ

80. SURA 'ABASA

Imeteremshwa Makka

Ina Aya 43 pamoja na Bismillahi

بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ ①

1. Kwa jina la Allah, Mwingi wa rehema, Mwingi wa ukarimu.

عَبَسَ وَتَوَلّٰٓى ②

2. Alikunja kipaji na akageuza uso,

اَنْ جَآءَهُ الْاَعْمٰى ③

3. Kwa sababu alimjia kipofu,

وَمَا يُدْرِيْكَ لَعَلَّهٗ يَزَّكّٰٓى ④

4. Na nini kikujulishe kwamba kulikuwa na uwezekano wa yeye kuwa mwenye kutakasika sana?

اَوْ يَذَّكَّرُ فَتَنْفَعَهُ الذِّكْرٰى ⑤

5. Au kama angezitafakari nasaha basi nasaha hizo zingempatia faida?

اَمَّا مَنِ اسْتَغْنٰى ⑥

6. Ama yule ambaye hakujali,

فَاَنْتَ لَهٗ تَصَدّٰى ⑦

7. Basi huyo ndiye unayemuelekea,

Sura hii ni katika sura za mwanzo zilizoshuka Makka.

Aya 2. *Alikunja kipaji,* yaani Mtume *s.a.w.* Siku moja alikuwa anawahubiria wakubwa wa Makka, na bwana mmoja kipofu, Abdullah bin Ummi Maktum alimkuta Mtume *s.a.w* anahubiri na akamsikia anaeleza, lakini juu ya hayo akataka Mtume amsikilize yeye. Jambo hili lilikuwa kinyume na adabu. Lakini Mtume kwa tabia yake nzuri asimkaripie neno ila tu akakunja uso. Padre Dale anasema kuwa Mtume "hapa anakiri kosa lake la kuwa na upendeleo na la kuangalia cheo cha watu." Maneno ya sura hii hayaonyeshi kosa lo lote linalokiriwa wala hakuna upendeleo na kuangalia vyeo. Maana Abdullah bin Ummi Maktum ilikuwa mahali pake asubiri mpaka amalize ndipo naye amwulize. Kadhalika Abdullah bin Ummi Maktum hakuwa mtu mdogo, yeye alikuwa mtoto wa kaka ya Khadija aliyekuwa mke wa Mtume s.a.w. na mara mbili Mtume s.a.w. alipoondoka kwa safari alimwacha Abdullah bin Ummi Maktum kuwa mkubwa wa Madina. Hivyo shauri ya kutazama vyeo hakuna hapa.

Hapa tutafananisha kisa hiki na kisa kimoja cha Yesu: "Mwanamke Mkananayo wa mipaka ile akatokea, akampaazia (Yesu) sauti akisema, Unirehemu bwana, mwana wa Daudi, binti yangu amepagawa sana na pepo. *Wala yeye hakumjibu neno* . . . (mwanamke) akaja akamsujudia, akisema, Bwana, unisaidie. Akajibu akasema, Si vema kukitwaa chakula cha watoto na *kuwatupia mbwa."* (*Watoto* ndio Waisraeli na *mbwa* ndiye mwanamke na wasio Waisraeli). Linganisha majibu haya ya Bwana Yesu na tabia ile bora ya Mtume *s.a.w.* nawe utaona kuna tofauti kubwa kati ya haya mawili. Mapadre wangesalimika kama wangeona miamba iliyomo katika macho yao kabla ya kutafuta vibanzi katika macho ya watu wengine.

وَمَا عَلَيْكَ اَلَّا يَزَّكّٰى ﴿٨﴾

8. Ilhali si jukumu lako kama yeye hakutakasika.

وَاَمَّا مَنْ جَآءَكَ يَسْعٰى ﴿٩﴾

9. Na yule aliyekujia kwa jitihada kubwa sana,

وَهُوَ يَخْشٰى ﴿١٠﴾

10. Naye alikuwa anaogopa,

فَاَنْتَ عَنْهُ تَلَهّٰى ﴿١١﴾

11. Basi huyo ukaghafilika naye.

كَلَّاۤ اِنَّهَا تَذْكِرَةٌ ﴿١٢﴾

12. Tahadhari! Hakika hii ni nasaha kubwa.

فَمَنْ شَآءَ ذَكَرَهٗ ﴿١٣﴾

13. Basi kila apendaye aikumbuke,

فِيْ صُحُفٍ مُّكَرَّمَةٍ ﴿١٤﴾

14. Katika kurasa zilizoheshimiwa.

مَّرْفُوْعَةٍ مُّطَهَّرَةٍ ﴿١٥﴾

15. Zilizonyanyuliwa zilizotakaswa,

بِاَيْدِيْ سَفَرَةٍ ﴿١٦﴾

16. Mikononi mwa waandishi.

كِرَامٍۭ بَرَرَةٍ ﴿١٧﴾

17. Watukufu watawa.

قُتِلَ الْاِنْسَانُ مَاۤ اَكْفَرَهٗ ﴿١٨﴾

18. Aangamizwe mtu! Ni asiyekuwa na shukrani kiasi gani!

مِنْ اَيِّ شَيْءٍ خَلَقَهٗ ﴿١٩﴾

19. Kwa kitu gani Amemwumba?

مِنْ نُّطْفَةٍ ؕ خَلَقَهٗ فَقَدَّرَهٗ ﴿٢٠﴾

20. Kwa tone la shahawa; Alim-wumba na Akamwekea mpangilio.

ثُمَّ السَّبِيْلَ يَسَّرَهٗ ﴿٢١﴾

21. Kisha akamfanyia njia kuwa nyepesi,

ثُمَّ اَمَاتَهٗ فَاَقْبَرَهٗ ﴿٢٢﴾

22. Kisha Akamfisha na Akam-wingiza kaburini,

ثُمَّ اِذَا شَآءَ اَنْشَرَهٗ ﴿٢٣﴾

23. Kisha Apendapo Atamfufua.

كَلَّا لَمَّا يَقْضِ مَاۤ اَمَرَهٗ ﴿٢٤﴾

24. Zingatia! hadi sasa hajaweza kuyatimiza yale aliyomuamuru.

فَلْيَنْظُرِ الْاِنْسَانُ اِلٰى طَعَامِهٖۤ ﴿٢٥﴾

25. Basi mtu atazame chakula chake.

اَنَّا صَبَبْنَا الْمَآءَ صَبًّا ﴿٢٦﴾

26. Hakika Tumemimina maji sana.

ثُمَّ شَقَقْنَا الْاَرْضَ شَقًّا ﴿٢٧﴾

27. Tena Tukaipasua-pasua ardhi,

فَاَنْۢبَتْنَا فِيْهَا حَبًّا ﴿٢٨﴾

28. Kisha Tukaziotesha humo mbegu,

وَّعِنَبًا وَّقَضْبًا ﴿٢٩﴾

29. Na mizabibu na mboga,

وَّزَيْتُوْنًا وَّنَخْلًا ﴿٣٠﴾

30. Na mizeituni na mitende.

وَّحَدَآئِقَ غُلْبًا ﴿٣١﴾

31. Na bustani zenye miti isonganayo,

وَّفَاكِهَةً وَّاَبًّا ﴿٣٢﴾

32. Na matunda na malisho.

مَّتَاعًا لَّكُمْ وَلِاَنْعَامِكُمْ ﴿٣٣﴾

33. Kuwafaidieni ninyi na wanyama wenu.

فَاِذَا جَآءَتِ الصَّآخَّةُ ﴿٣٤﴾

34. Basi itakapokuja sauti kali ivunjayo masikio,

يَوْمَ يَفِرُّ الْمَرْءُ مِنْ اَخِيْهِ ﴿٣٥﴾

35. Siku ambayo mtu atamkimbia nduguye.

وَاُمِّهٖ وَاَبِيْهِ ﴿٣٦﴾

36. Na mamaye na babaye,

وَصَاحِبَتِهٖ وَبَنِيْهِ ﴿٣٧﴾

37. Na mkewe na mwanawe -

لِكُلِّ امْرِئٍ مِّنْهُمْ يَوْمَئِذٍ شَاْنٌ يُّغْنِيْهِ ﴿٣٨﴾

38. Kila mtu miongoni mwao siku hiyo atakuwa na hali itakayomtosha.

وُجُوْهٌ يَّوْمَئِذٍ مُّسْفِرَةٌ ﴿٣٩﴾

39. Siku hiyo nyuso zitanawiri.

ضَاحِكَةٌ مُّسْتَبْشِرَةٌ ﴿٤٠﴾

40. Zitacheka, zitachangamka.

وَوُجُوْهٌ يَّوْمَئِذٍ عَلَيْهَا غَبَرَةٌ ﴿٤١﴾

41. Na nyuso Siku hiyo zitakuwa na mavumbi juu yao,

تَرْهَقُهَا قَتَرَةٌ ﴿٤٢﴾

42. Giza zito litazifunika.

اُولٰٓئِكَ هُمُ الْكَفَرَةُ الْفَجَرَةُ ﴿٤٣﴾

43. Hao ndio makafiri, waovu.

سُوْرَةُ التَّكْوِيْرِ مَكِّيَّةٌ وَّ هِيَ مَعَ الْبَسْمَلَةِ ثَلَاثُوْنَ اٰيَةً وَّ رُكُوْعٌ

81. SURA AT-TAKWIIR

Imeteremshwa Makka

Ina Aya 30 pamoja na Bismillahi

بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ ①

1. Kwa jina la Allah, Mwingi wa rehema, Mwingi wa ukarimu.

اِذَا الشَّمْسُ كُوِّرَتْ ۖ ②

2. Jua litakapofunikwa,

وَ اِذَا النُّجُوْمُ انْكَدَرَتْ ۖ ③

3. Na nyota zitakapotiwa giza,

وَ اِذَا الْجِبَالُ سُيِّرَتْ ۖ ④

4. Na milima itakapotembezwa,

وَ اِذَا الْعِشَارُ عُطِّلَتْ ۖ ⑤

5. Na ngamia watakapoachwa,

وَ اِذَا الْوُحُوْشُ حُشِرَتْ ۖ ⑥

6. Na wanyama wa mwitu watakapokusanywa,

وَ اِذَا الْبِحَارُ سُجِّرَتْ ۖ ⑦

7. Na bahari zitakapopasuliwa,

وَ اِذَا النُّفُوْسُ زُوِّجَتْ ۖ ⑧

8. Na nafsi zitakapounganishwa,

وَ اِذَا الْمَوْءٗدَةُ سُئِلَتْ ۖ ⑨

9. Na msichana aliyezikwa hai atakapoulizwa:

Sura hii ilishuka Makka. Kwa kuitaja sura hii Mtume *s.a.w.* alisema, "Anayetaka kujua Kiyama kama kitu kinachoonekana kwa macho, basi asome *Idhaa-s-samaaun shaqqat, Idha-s-samaaun fatarat* na *Idhash-shams kuwwirat* (Ruhul Ma'aani). Kadhalika Hadithi hii imesimuliwa katika Musnad Ahmad bin hanbal. Hadithi hii pia inajulisha ya kuwa sura hizi zinaeleza habari za siku ya Kiyama.

Aya 2-4. Katika Aya hizi mmeelezwa alama za akheri zamani, yaani mambo yatakayotokea katika siku za mwisho. Jua kufunikwa ni mafundisho ya Kiislamu hayatajulikana na hayatafuatwa na watu, na pia yatafunikwa na upinzani wa watu hata uzuri wake ufichike.
Mtume *s.a.w.* alisema: "Hakutabaki katika Uislamu ila jina tu, wala hakutabaki katika Qur'an ila maandishi tu, misikiti yao itakuwa mikubwa lakini haitakuwa na mwongozo, masheikh na waalimu wao watakuwa ndio wabaya zaidi chini ya mbingu" (Bukhari). Nyota ni Masheikh na waalimu, wakati huo hawatakuwa na ucha-Mungu na elimu yao itaingia giza, na haitawafaa watu. Majabali kuondolewa ni watu wakubwa-wakubwa au majabali yenyewe yataondoka kama tuonavyo siku hizi. Ngamia watakapoachwa maana yake siku hizo njia mpya za kusafiria na za uchukuzi zitavumbuliwa na watu hawatatumia ngamia. Wanyama kukusanywa mradi wake ni namna mbili: (1) watu wasiostaarabika watakapopatiwa njia za kuwastaarabisha; (2) wanyama wa mwitu watakusanywa pamoja kama tuonavyo katika ma-"zoo" ambayo humo wamekusanywa wanyama

بِاَيِّ ذَنۢبٍ قُتِلَتۡ ۚ﴿٩﴾

10. Kwa kosa gani aliuawa?

وَاِذَا الصُّحُفُ نُشِرَتۡ ۚ﴿١٠﴾

11. Na sahifa zitakapoenezwa,

وَاِذَا السَّمَآءُ كُشِطَتۡ ۚ﴿١١﴾

12. Na utando wa mbingu utakapotanduliwa,

وَاِذَا الۡجَحِيۡمُ سُعِّرَتۡ ۚ﴿١٢﴾

13. Na Jahanamu itakapokokwa,

وَاِذَا الۡجَنَّةُ اُزۡلِفَتۡ ۚ﴿١٣﴾

14. Na Pepo itakaposogezwa,

عَلِمَتۡ نَفۡسٌ مَّاۤ اَحۡضَرَتۡ ؕ﴿١٤﴾

15. (Wakati huo) nafsi itajua ilichokihudhurisha.

فَلَاۤ اُقۡسِمُ بِالۡخُنَّسِ ۙ﴿١٥﴾

16. Hivyo tahadhari! Naapa kwa warudiao nyuma baada ya kufanya njama za siri,

الۡجَوَارِ الۡكُنَّسِ ۙ﴿١٦﴾

17. Merikebu zenye kujificha wakati wa kujificha,

وَالَّيۡلِ اِذَا عَسۡعَسَ ۙ﴿١٧﴾

18. Na kwa usiku utakapokuja na kuondoka,

وَالصُّبۡحِ اِذَا تَنَفَّسَ ۙ﴿١٨﴾

19. Na kwa asubuhi itakapopambazuka,

اِنَّهٗ لَقَوۡلُ رَسُوۡلٍ كَرِيۡمٍ ۙ﴿١٩﴾

20. Kwa hakika hii ni kauli ya Mtume mtukufu,

ذِىۡ قُوَّةٍ عِنۡدَ ذِى الۡعَرۡشِ مَكِيۡنٍ ۙ﴿٢٠﴾

21. Mwenye nguvu, mwenye cheo cha heshima Mwenye enzi,

مُّطَاعٍ ثَمَّ اَمِيۡنٍ ؕ﴿٢١﴾

22. Anayetiiwa kisha mwaminifu.

---

wa kila namna wa porini. Mito kupasuliwa ni kwamba mifereji ya maji itatolewa ndani ya mito mikubwa mikubwa na maji yake kumwagiwa mashamba. Na pia bahari zitapasuliwa ili ziunganishwe kama zilivyounganishwa pamoja kwa mifereji ya Panama na Suez. Watu kuunganishwa na kama tuonavyo watu wanavyojikusanya pamoja hali zamani wakikaa mbalimbali, na pia kwa vyombo vya dunia siku hizi watu wote wamekutanishwa. Desturi ya kuzika wanawake hai walivyokuwa wakifanya watu katika siku za ushenzi itazuiliwa. Vitabu kuenezwa ni wazi kabisa siku hizi tunapoona malaki kwa malaki ya magazeti na vitabu kutangazwa. Watu watafanya bidii kujua habari za angani na za vitu vya mbinguni na uvumbuzi wa ajabu utafanyika na watu wataruka huko na huko mbinguni. Mambo ya anasa yatakuwa mengi hata Jahanamu itawasogelea watu karibu karibu na pia Pepo itasogea karibu sana kwa watakaofanya bidii kuepuka maovu, hata Mtume *s.a.w.* alisema, mtu anayeshika suna zake katika umati wa watu wabaya atapata ujira wa mashahidi mia.

Bishara hizi zinazoelezwa hapa na katika sura zifuatazo, zilibashiriwa toka miaka 1,300 iliyopita, na namna zinavyotimia zinaonyesha waziwazi kuwa Kitabu cha Qur'an kimetoka kwa Allah na mafundisho yake yote ni ya kweli na watakaoyafuata bila shaka watafanikiwa.

وَمَا صَاحِبُكُمْ بِمَجْنُوْنٍ ﴿٢٢﴾

23. Na mwezenu si mwenda wazimu.

وَلَقَدْ رَاٰهُ بِالْاُفُقِ الْمُبِيْنِ ﴿٢٣﴾

24. Na hakika yeye alimwona kwenye upeo wa macho ulio safi.

وَمَا هُوَ عَلَى الْغَيْبِ بِضَنِيْنٍ ﴿٢٤﴾

25. Wala yeye si bahili kueleza mambo ya ghaibu.

وَمَا هُوَ بِقَوْلِ شَيْطٰنٍ رَّجِيْمٍ ﴿٢٥﴾

26. Wala hii si kauli ya Shetani afukuzwaye.

فَاَيْنَ تَذْهَبُوْنَ ﴿٢٦﴾

27. Basi mnakwenda wapi?

اِنْ هُوَ اِلَّا ذِكْرٌ لِّلْعٰلَمِيْنَ ﴿٢٧﴾

28. Hiyo siyo ila ni nasaha kubwa kwa walimwengu,

لِمَنْ شَآءَ مِنْكُمْ اَنْ يَّسْتَقِيْمَ ﴿٢٨﴾

29. Kwa yule miongoni mwenu apendaye kushika njia iliyonyooka.

وَمَا تَشَآءُوْنَ اِلَّآ اَنْ يَّشَآءَ اللّٰهُ رَبُّ الْعٰلَمِيْنَ ﴿٢٩﴾ ع

30. Wala ninyi hamtapenda isipokuwa Apende Allah, Mola wa walimwengu.

سُوْرَةُ الْاِنْفِطَارِ مَكِّيَّةٌ وَّ هِيَ مَعَ الْبَسْمَلَةِ عِشْرُوْنَ اٰيَةً وَّ رُكُوْعٌ

82. SURA AL-INFITAAR

Imeteremshwa Makka

Ina Aya 20 pamoja na Bismillahi

بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ ①

1. Kwa jina la Allah, Mwingi wa rehema, Mwingi wa ukarimu.

اِذَا السَّمَآءُ انْفَطَرَتْ ۙ ②

2. Mbingu itakapopasuka,

وَ اِذَا الْكَوَاكِبُ انْتَثَرَتْ ۙ ③

3. Na nyota zitakapotawanyika,

وَ اِذَا الْبِحَارُ فُجِّرَتْ ۙ ④

4. Na bahari zitakapopasuliwa,

وَ اِذَا الْقُبُوْرُ بُعْثِرَتْ ۙ ⑤

5. Na makaburi yatakapofukuliwa,

عَلِمَتْ نَفْسٌ مَّا قَدَّمَتْ وَ اَخَّرَتْ ؕ ⑥

6. Nafsi itajua iliyoyatanguliza na iliyoyabakisha nyuma.

يٰۤاَيُّهَا الْاِنْسَانُ مَا غَرَّكَ بِرَبِّكَ الْكَرِيْمِ ۙ ⑦

7. Ee mwanadamu! ni nini kikudanganyacho na Mola wako Mkarimu?

الَّذِيْ خَلَقَكَ فَسَوّٰىكَ فَعَدَلَكَ ۙ ⑧

8. Aliyekuumba na kukustawisha, kisha Akakulinganisha sawa?

فِيْۤ اَيِّ صُوْرَةٍ مَّا شَآءَ رَكَّبَكَ ؕ ⑨

9. Katika sura yo yote Aliyoipenda Amekutengeneza.

كَلَّا بَلْ تُكَذِّبُوْنَ بِالدِّيْنِ ۙ ⑩

10. Siyo! Bali ninyi mnaikadhibisha siku ya Hukumu,

Sura hii ilishuka Makka. Jina lake limetoka katika Aya ya 2 inayoeleza kupasuka kwa mbingu (Tazama sura 81).

Aya 5. Makaburi kufukuliwa inaweza kuwa na muradi wa makaburi ya zamani yanayofukuliwa siku hizi kwa ajili ya kutafuta kujua habari za watu wa kale.

Aya 7. Kuna baadhi ya watu ambao hudhani si neno wakiendelea kufanya dhambi: Mungu ni Mkarimu, atawasamehe. Hapa wanaambiwa kufikiri hivi ni kudanganyika, maana Mungu pia ni mkali wa kuadhibu. Wakristo hasa huwa na dhana hii wakifikiri hawana dhambi ati Yesu amekwisha wakomboa kwa kuwa alikufa kwa ajili yao. Allah amesema, "*Waambie watumishi Wangu ya kwamba Mimi ni Msamehevu, Mrehemevu. Na hakika adhabu Yangu ndiyo adhabu iumizayo"* (sura 15:50-51).

وَاِنَّ عَلَيْكُمْ لَحٰفِظِيْنَ ﴿١١﴾

11. Na hakika juu yenu kuna walinzi,

كِرَامًا كَاتِبِيْنَ ﴿١٢﴾

12. Waandishi wenye heshima,

يَعْلَمُوْنَ مَا تَفْعَلُوْنَ ﴿١٣﴾

13. Wanajua mnayoyatenda.

اِنَّ الْاَبْرَارَ لَفِيْ نَعِيْمٍ ﴿١٤﴾

14. Kwa hakika wafanyao wema watakuwa neemani.

وَاِنَّ الْفُجَّارَ لَفِيْ جَحِيْمٍ ﴿١٥﴾

15. Na kwa hakika waovu watakuwa Motoni,

يَّصْلَوْنَهَا يَوْمَ الدِّيْنِ ﴿١٦﴾

16. Wataingia humo siku ya Malipo,

وَمَا هُمْ عَنْهَا بِغَآئِبِيْنَ ﴿١٧﴾

17. Wala hawataweza kufanya wasiwemo humo.

وَمَآ اَدْرٰىكَ مَا يَوْمُ الدِّيْنِ ﴿١٨﴾

18. Na nini kitakujulisha siku ya Malipo ni nini?

ثُمَّ مَآ اَدْرٰىكَ مَا يَوْمُ الدِّيْنِ ﴿١٩﴾

19. Tena nini kitakujulisha siku ya Malipo ni nini?

يَوْمَ لَا تَمْلِكُ نَفْسٌ لِّنَفْسٍ شَيْـًٔا ؕ وَالْاَمْرُ يَوْمَئِذٍ لِّلّٰهِ ﴿٢٠﴾ ع

20. (Ni) Siku ambayo nafsi haitamilikia nafsi (nyingine) cho chote; na amri Siku hiyo itakuwa ya Allah.

سُوْرَةُ الْمُطَفِّفِيْنَ مَكِّيَّةٌ وَّ هِيَ مَعَ الْبَسْمَلَةِ سَبْعٌ وَّ ثَلَا ثُوْنَ اٰيَةً وَّ رُكُوْعٌ

83. SURA AL-MUTAFFIFIIN

Imeteremshwa Makka

Ina Aya 37 pamoja na Bismillahi

بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ ①

1. Kwa jina la Allah, Mwingi wa rehema, Mwingi wa ukarimu.

وَيْلٌ لِّلْمُطَفِّفِيْنَ ②

2. Maangamizo kwa wapunjao!

الَّذِيْنَ اِذَا اكْتَالُوْا عَلَى النَّاسِ يَسْتَوْفُوْنَ ③

3. Ambao wanapojipimia kwa watu hupokea (kipimo) kamili;

وَ اِذَا كَالُوْهُمْ اَوْ وَّزَنُوْهُمْ يُخْسِرُوْنَ ④

4. Lakini wanapowapimia kwa kipimo au mizani, wao hupunguza.

اَلَا يَظُنُّ اُولٰٓئِكَ اَنَّهُمْ مَّبْعُوْثُوْنَ ⑤

5. Je! wao hawafikiri ya kwamba watafufuliwa,

لِيَوْمٍ عَظِيْمٍ ⑥

6. Katika Siku iliyo kuu,

يَّوْمَ يَقُوْمُ النَّاسُ لِرَبِّ الْعٰلَمِيْنَ ⑦

7. Siku watakaposimama watu mbele ya Mola wa walimwengu?

كَلَّآ اِنَّ كِتٰبَ الْفُجَّارِ لَفِيْ سِجِّيْنٍ ⑧

8. Sikilizeni! Kwa hakika daftari ya waovu imo ndani ya Sijjiin.

وَمَآ اَدْرٰىكَ مَا سِجِّيْنٌ ⑨

9. Na nini kitakujulisha Sijjiin ni nini?

كِتٰبٌ مَّرْقُوْمٌ ⑩

10. (Ni) kitabu kilichoandikwa.

وَيْلٌ يَّوْمَئِذٍ لِّلْمُكَذِّبِيْنَ ⑪

11. Ole Siku hiyo kwa wanaokadhibisha,

Wafasiri wanahitilafiana juu ya sura hii. Wengine wanasema ilishuka Madina. Lakini wengi zaidi wanakubali ya kuwa ilishuka Makka. Imepewa jina lake toka Aya ya 2 inayoapiza watu wanaopunja katika vipimo na mizani.

Aya 2. *Mutaffifiin,* "Wapunjao." Aya hii inawaonya sana watu wafanyao biashara ambao wanapopokea vitu wanavyonunua kwa watu wanachukua kipimo kamili, lakini wakiwapimia watu, wanawapunja. Kadhalika kila upungufu katika wajibu wa mtu ni kupunja kunakolaumiwa na Aya hii. Siku moja Seyidna Umar alimwuliza mtu mmoja aliyechelewa kusali. Mtu yule akatoa udhuru wake. Seyidna Umar akamwambia. *"Tafafta"* yaani umepunguza.

الَّذِيْنَ يُكَذِّبُوْنَ بِيَوْمِ الدِّيْنِ ﴿١٢﴾

12. Ambao wanaikadhibisha siku ya hukumu.

وَمَا يُكَذِّبُ بِهٖٓ اِلَّا كُلُّ مُعْتَدٍ اَثِيْمٍ ﴿١٣﴾

13. Wala haikadhibishi ila kila mwenye kuruka mipaka, mwenye dhambi;

اِذَا تُتْلٰى عَلَيْهِ اٰيٰتُنَا قَالَ اَسَاطِيْرُ الْاَوَّلِيْنَ ﴿١٤﴾

14. Anaposomewa Aya Zetu, husema; Ni visa vya watu wa kale.

كَلَّا بَلْ ۜ رَانَ عَلٰى قُلُوْبِهِمْ مَّا كَانُوْا يَكْسِبُوْنَ ﴿١٥﴾

15. Zingatia! Ukweli ndio huu kwamba yametia kutu juu ya nyoyo zao matendo waliyokuwa wakiyatenda.

كَلَّآ اِنَّهُمْ عَنْ رَّبِّهِمْ يَوْمَئِذٍ لَّمَحْجُوْبُوْنَ ﴿١٦﴾

16. Zingatia! Hakika kwa Mola wao, Siku hiyo, watakingiwa pazia.

ثُمَّ اِنَّهُمْ لَصَالُوا الْجَحِيْمِ ﴿١٧﴾

17. Kisha wao lazima wataingia ndani ya Jahannam.

ثُمَّ يُقَالُ هٰذَا الَّذِيْ كُنْتُمْ بِهٖ تُكَذِّبُوْنَ ﴿١٨﴾

18. Kisha wataambiwa: Haya ndiyo mliyokuwa mkiyakadhibisha.

كَلَّآ اِنَّ كِتٰبَ الْاَبْرَارِ لَفِيْ عِلِّيِّيْنَ ﴿١٩﴾

19. Sivyo (mnavyodhani)! Hakika kitabu cha matendo ya watawa kipo kwenye illiyyiin.

وَمَآ اَدْرٰىكَ مَا عِلِّيُّوْنَ ﴿٢٠﴾

20. Na nini kitakujulisha illiyyiin ni nini?

كِتٰبٌ مَّرْقُوْمٌ ﴿٢١﴾

21. (Ni) kitabu kilichoandikwa.

يَّشْهَدُهُ الْمُقَرَّبُوْنَ ﴿٢٢﴾

22. Watakiona (kwa macho yao) walio karibu (na Allah).

اِنَّ الْاَبْرَارَ لَفِيْ نَعِيْمٍ ﴿٢٣﴾

23. Hakika wafanyao wema watakuwa kwenye neema,

عَلَى الْاَرَآئِكِ يَنْظُرُوْنَ ﴿٢٤﴾

24. Wakikaa juu ya viti vya fahari wakiangaza;

تَعْرِفُ فِيْ وُجُوْهِهِمْ نَضْرَةَ النَّعِيْمِ ﴿٢٥﴾ ۚ

25. Utatambua marini ya neema katika nyuso zao.

يُسْقَوْنَ مِنْ رَّحِيْقٍ مَّخْتُوْمٍ ﴿٢٦﴾

26. Watanyweshwa kinywaji halisi chenye muhuri;

خِتٰمُهٗ مِسْكٌ ۭ وَفِيْ ذٰلِكَ فَلْيَتَنَافَسِ الْمُتَنَافِسُوْنَ ﴿٢٧﴾

27. Muhuri wake ni miski; na hicho watamanio watakitamani sana.

وَمِزَاجُهٗ مِنْ تَسْنِيْمٍ ﴿٢٨﴾

28. Na mchanganyiko wake ni (maji ya) Tasnim,

عَيْنًا يَّشْرَبُ بِهَا الْمُقَرَّبُوْنَ ﴿٢٩﴾

29. Ni chemchem watainywa (watu) walio karibu (na Allah),

30. Kwa hakika wale waliokosa walikuwa wakiwacheka walioamini;

اِنَّ الَّذِيْنَ اَجْرَمُوْا كَانُوْا مِنَ الَّذِيْنَ اٰمَنُوْا يَضْحَكُوْنَ ۝٢٩

31. Na walipopita karibu yao walikonyezana;

وَاِذَا مَرُّوْا بِهِمْ يَتَغَامَزُوْنَ ۝٣٠

32. Na waliporudi kwa ahali zao walirudi wakisema upuuzi.

وَاِذَا انْقَلَبُوْٓا اِلٰٓى اَهْلِهِمُ انْقَلَبُوْا فَكِهِيْنَ ۝٣١

33. Na walipowaona walisema, Hakika hao ndio hasa waliopotea.

وَاِذَا رَاَوْهُمْ قَالُوْٓا اِنَّ هٰٓؤُلَآءِ لَضَآلُّوْنَ ۝٣٢

34. Na wao hawakupelekwa kuwa walinzi juu yao.

وَمَآ اُرْسِلُوْا عَلَيْهِمْ حٰفِظِيْنَ ۝٣٣

35. Basi leo walioamini watawacheka waliokufuru;

فَالْيَوْمَ الَّذِيْنَ اٰمَنُوْا مِنَ الْكُفَّارِ يَضْحَكُوْنَ ۝٣٤

36. (Watakuwa) juu ya viti vya fahari wakiangaza.

عَلَى الْاَرَآئِكِ يَنْظُرُوْنَ ۝٣٥

37. Je, makafiri wamepewa malipo ya yale waliyokuwa wakiyatenda?

هَلْ ثُوِّبَ الْكُفَّارُ مَا كَانُوْا يَفْعَلُوْنَ ۝٣٦

سُوْرَةُ الاِنْشِقَاقِ مَكِّيَّةٌ وَّ هِيَ مَعَ الْبَسْمَلَةِ سِتٌّ وَّ عِشْرُوْنَ اٰيَةً وَّ رُكُوْعٌ

84. SURA AL-INSHIQAAQ

Imeteremshwa Makka

Ina Aya 26 pamoja na Bismillahi

بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ ①

1. Kwa jina la Allah, Mwingi wa rehema, Mwingi wa ukarimu.

اِذَا السَّمَآءُ انْشَقَّتْ ۙ ②

2. Mbingu itakapopasuka

وَ اَذِنَتْ لِرَبِّهَا وَ حُقَّتْ ۙ ③

3. Na kukinga sikio kwa Mola wake na imeipasa (kusikia).

وَ اِذَا الْاَرْضُ مُدَّتْ ۙ ④

4. Na ardhi itakapotanuliwa,

وَ اَلْقَتْ مَا فِيْهَا وَ تَخَلَّتْ ۙ ⑤

5. Na kuvitoa vilivyomo na kuwa tupu,

وَ اَذِنَتْ لِرَبِّهَا وَ حُقَّتْ ۭ ⑥

6. Na kukinga sikio kwa Mola wake na imeipasa (kusikia).

يٰۤاَيُّهَا الْاِنْسَانُ اِنَّكَ كَادِحٌ اِلٰى رَبِّكَ كَدْحًا فَمُلٰقِيْهِ ۚ ⑦

7. Ewe mtu, hakika wewe ndiwe ufanyaye juhudi sana kwa Mola wako, basi utakutana naye.

فَاَمَّا مَنْ اُوْتِيَ كِتٰبَهٗ بِيَمِيْنِهٖ ۙ ⑧

8. Ama atakayepewa kitabu chake cha matendo kwa mkono wake wa kulia,

فَسَوْفَ يُحَاسَبُ حِسَابًا يَّسِيْرًا ۙ ⑨

9. Basi yeye atahesabiwa hesabu rahisi,

وَّ يَنْقَلِبُ اِلٰۤى اَهْلِهٖ مَسْرُوْرًا ۭ ⑩

10. Na atarudi kwa ahali zake mwenye furaha.

وَ اَمَّا مَنْ اُوْتِيَ كِتٰبَهٗ وَرَآءَ ظَهْرِهٖ ۙ ⑪

11. Lakini atakayepewa kitabu chake cha matendo kwa nyuma ya mgongo wake,

فَسَوْفَ يَدْعُوْا ثُبُوْرًا ۙ ⑫

12. Basi yeye atajiombea maangamizo,

وَّ يَصْلٰى سَعِيْرًا ۭ ⑬

13. Na ataingia Motoni:

اِنَّهٗ كَانَ فِيْۤ اَهْلِهٖ مَسْرُوْرًا ۭ ⑭

14. Maana alikuwa anakaa na ahali zake kwa furaha.

Maneno na madhumuni ya sura hii yanaonyesha ya kwamba ilishuka Makka miongoni mwa sura za mwanzo. Sura hii imepata jina lake katika Aya ya 2 inayoeleza juu ya mbingu kupasuka.

15. Hakika alidhani kuwa hatafufuliwa kamwe.
16. Naam! Hakika Mola wake Alikuwa Akimwona.
17. Basi Ninaapa kwa wekundu wa jua lichwapo.
18. Na kwa usiku na unavyovikusanya.
19. Na kwa mwezi unapokomaa,
20. Lazima ninyi mtapata maendeleo hatua kwa hatua.
21. Basi wana nini hawaamini?
22. Na wanaposomewa Qur'an, hawasujudu.
23. Lakini wale waliokufuru wanakadhibisha.
24. Na Allah Anayajua sana wanayoyakusanya.
25. Basi wabashirie adhabu iumizayo,
26. Isipokuwa wale walioamini na waliotenda vitendo vizuri; watakuwa na ujira usio na kikomo.

إِنَّهُ ظَنَّ أَنْ لَّنْ يَّحُوْرَ ﴿١٥﴾ ۚ
بَلٰٓى ۚ إِنَّ رَبَّهُ كَانَ بِهٖ بَصِيْرًا ﴿١٦﴾ ۘ
فَلَآ أُقْسِمُ بِالشَّفَقِ ﴿١٧﴾ ۙ
وَالَّيْلِ وَمَا وَسَقَ ﴿١٨﴾ ۙ
وَالْقَمَرِ إِذَا اتَّسَقَ ﴿١٩﴾ ۙ
لَتَرْكَبُنَّ طَبَقًا عَنْ طَبَقٍ ﴿٢٠﴾ ۘ
فَمَا لَهُمْ لَا يُؤْمِنُوْنَ ﴿٢١﴾ ۙ
وَإِذَا قُرِئَ عَلَيْهِمُ الْقُرْاٰنُ
لَا يَسْجُدُوْنَ ﴿٢٢﴾ ۩
بَلِ الَّذِيْنَ كَفَرُوْا يُكَذِّبُوْنَ ﴿٢٣﴾ ۙ
وَاللّٰهُ أَعْلَمُ بِمَا يُوْعُوْنَ ﴿٢٤﴾ ۚ
فَبَشِّرْهُمْ بِعَذَابٍ أَلِيْمٍ ﴿٢٥﴾ ۙ
إِلَّا الَّذِيْنَ اٰمَنُوْا وَعَمِلُوا الصّٰلِحٰتِ
لَهُمْ أَجْرٌ غَيْرُ مَمْنُوْنٍ ﴿٢٦﴾ ع

سُوْرَةُ الْبُرُوْجِ مَكِّيَّةٌ وَّ هِيَ مَعَ الْبَسْمَلَةِ ثَلَاثٌ وَّ عِشْرُوْنَ اٰيَةً وَّ رُكُوْعٌ

85. SURA AL-BURUUJ

Imeteremshwa Makka

Ina Aya 23 pamoja na Bismillahi

بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ ①

1. Kwa jina la Allah, Mwingi wa rehema, Mwingi wa ukarimu.

وَالسَّمَآءِ ذَاتِ الْبُرُوْجِ ②

2. Naapa kwa mbingu yenye nyota.

وَالْيَوْمِ الْمَوْعُوْدِ ③

3. Na kwa siku ya miadi,

وَشَاهِدٍ وَّمَشْهُوْدٍ ④

4. Na kwa shahidi na kwa anayeshuhudiwa.

قُتِلَ اَصْحٰبُ الْاُخْدُوْدِ ⑤

5. Wataangamizwa watu wa mahandaki.

النَّارِ ذَاتِ الْوَقُوْدِ ⑥

6. (Yaani) watu wenye moto ulio na kuni nyingi,

Sura hii ilishuka Makka, na wafasiri wanakiri ya kuwa hakuna hitilafu juu ya jambo hili.

Aya 2. *Buruuj.* Neno hili ni wingi wa neno *Burj,* na maana zake ni "sehemu madhubuti ya jengo" (kama nguzo): "ngome"; "jumba kubwa"; pia mahali pa mazunguko ya nyota panaitwa *Buruuj* (Akrab).

Aya 5. *Ukhduud.* Neno hili maana yake ni shimo refu lililochimbwa katika ardhi, yaani handaki (Akrab).

Wafasiri wa zamani wameandika ya kuwa *As-haabul-ukhduud* ni watu waliokuwa wakimwabudu Allah ambao mfalme wa nchi ya Habeshi aliwatia taabuni; au wanasema , ni Nabii Daniel pamoja na wenzake wawili ambao kwa sababu ya kumwabudu Allah wakatiwa katika tanuru la moto na mfalme Nebuchadnezar. Ingawa ni kweli ya kuwa watu watatu walitupwa ndani ya tanuru la moto lakini Daniel hakuwemo katika watu hao.

Lakini kwa kuwa habari za sura hii zinaeleza mambo yatakayokuja akheri zamani ni dhahiri ya kwamba taabu hizi zilizoelezwa hapa watazipata wale watakaoingia kueneza dini ya Kiislamu. Na Seyidna Ahmad a.s. amesema kuwahimiza wafuasi wake ya kuwa mwendeleo wa Uislamu unataka mauti. Naye ametoa bishara na kusema, "Ushindi wa ukweli utatokea. Na siku ya upya na mng'ao wa Uislamu itakuja kama ilivyokuja zamani. Na jua la Kiislamu litang'aa kwa ukamilifu kama lilivyong'aa kwanza, lakini bado. Naam, mbingu imelizuia lisionekane mpaka moyo wetu kwa juhudi na mashaka usagike na raha zote tuzipoteze ili lipate kung'aa, hata tukubali fedheha ya kila namna kwa ajili ya heshima ya Uislamu. Uhai wa Uislamu unatutaka fidia. Fidia hiyo ni nini? Ni kwamba tufe katika njia hii hii. Ndicho kifo ambacho unategemea uhai wa Islamu na uhai wa Waislamu na maonyesho ya Allah Aliye hai (Fat'hi Islam, uk. 14-16).

إِذْ هُمْ عَلَيْهَا قُعُودٌ ۝٧

Watakapokuwa wameketi pembezoni mwake.

وَّهُمْ عَلٰى مَا يَفْعَلُوْنَ بِالْمُؤْمِنِيْنَ شُهُوْدٌ ۝٨

8. Nao watakuwa ni mashahidi wa yale watakayoyafanya kwa waaminio.

وَمَا نَقَمُوْا مِنْهُمْ اِلَّآ اَنْ يُّؤْمِنُوْا بِاللّٰهِ الْعَزِيْزِ الْحَمِيْدِ ۝٩

9. Nao hawawachukii ila kwa sababu wamemwamini Allah, Mwenye ushindi kamili, Mwenye kusifiwa.

الَّذِيْ لَهٗ مُلْكُ السَّمٰوٰتِ وَالْاَرْضِ ۭ وَاللّٰهُ عَلٰي كُلِّ شَيْءٍ شَهِيْدٌ ۝١٠

10. Ambaye ni Mwenye ufalme wa mbingu na ardhi; na Allah ni shahidi wa kila kitu.

اِنَّ الَّذِيْنَ فَتَنُوا الْمُؤْمِنِيْنَ وَالْمُؤْمِنٰتِ ثُمَّ لَمْ يَتُوْبُوْا فَلَهُمْ عَذَابُ جَهَنَّمَ وَلَهُمْ عَذَابُ الْحَرِيْقِ ۝١١

11. Hakika wale waliowafitini waaminio wanaume na waaminio wanawake, kisha hawakutubu, basi itakuwa kwao adhabu ya Jahanamu, na watapata adhabu ya kuungua.

اِنَّ الَّذِيْنَ اٰمَنُوْا وَعَمِلُوا الصّٰلِحٰتِ لَهُمْ جَنّٰتٌ تَجْرِيْ مِنْ تَحْتِهَا الْاَنْهٰرُ ۭ ذٰلِكَ الْفَوْزُ الْكَبِيْرُ ۝١٢

12. Hakika wale walioamini na kutenda vitendo vizuri bila shaka zitakuwa kwao Bustani zenye mito ipitayo ndani yake, hayo ni mafanikio makubwa sana.

اِنَّ بَطْشَ رَبِّكَ لَشَدِيْدٌ ۝١٣

13. Hakika mkamato wa Mola wako ni mkali sana.

اِنَّهٗ هُوَ يُبْدِئُ وَيُعِيْدُ ۝١٤

14. Hakika Yeye Ndiye Anayeanzisha na kurudisha.

وَهُوَ الْغَفُوْرُ الْوَدُوْدُ ۝١٥

15. Naye ni msamehevu, Mwenye upendo sana,

ذُو الْعَرْشِ الْمَجِيْدُ ۝١٦

16. Mwenye kiti cha enzi, Mtukufu,

Aya 12. *Kutenda vitendo vizuri.* Yaani wanaofanya vitendo vizuri mahali vinapohitajika. Hii ndio maana hasa ya kutenda wema. Mathalan, kufunga saumu ni kitendo chema, lakini kufunga saumu siku ya Idi ni kitendo cha Shetani.

Zitakuwa kwao Bustani zenye mito, ndio kusema, watapata neema namna mbili, za juu na chini: watapata raha ya mwili na ya roho, na wataheshimiwa na watu na pia Allah.

Aya 14. *Yubdiu wa yu'iidu.* Mradi wa maneno haya ni kuwa Allah ndiye atakayewaadhibu hapa duniani na atakayewaadhibu katika Akhera pia.

17. Atendaye Apendavyo. فَعَّالٌ لِّمَا يُرِيْدُ ﴿١٧﴾

18. Je, zimekuwasilia habari za majeshi, هَلْ اَتٰىكَ حَدِيْثُ الْجُنُوْدِ ﴿١٨﴾

19. Ya Firauni na ya Wathamudi? فِرْعَوْنَ وَثَمُوْدَ ﴿١٩﴾

20. Lakini waliokufuru wamo katika kukadhibisha. بَلِ الَّذِيْنَ كَفَرُوْا فِيْ تَكْذِيْبٍ ﴿٢٠﴾

21. Na Allah Amewazunguka kote. وَّاللّٰهُ مِنْ وَّرَآئِهِمْ مُّحِيْطٌ ﴿٢١﴾

22. Bali hii ni Qur'an tukufu, بَلْ هُوَ قُرْاٰنٌ مَّجِيْدٌ ﴿٢٢﴾

23. Katika ubao uliohifadhiwa. فِيْ لَوْحٍ مَّحْفُوْظٍ ﴿٢٣﴾

Aya 23. *Lauh* ni kila ubapa wa mti au mfupa. Muradi wa kusema kuwa Qur'an iko katika "ubao uliohifadhiwa" ni kuwa iko wazi na itaenea sana na itafika katika mikono ya watu wengi. Sasa kitu kilicho wazi na kinachofika mbali mikononi mwa watu mbalimbali mtu atafikiri ya kuwa kitu cha namna hiyo kinaweza kuharibika. Basi Aya hii inaondoa shaka hiyo na kusema kuwa pia imehifadhika, na ya kwamba juu ya kuenea kwake namna hiyo watu hawataweza kuigeuza au kuibadilisha na kuiharibu, na itakaa salama kabisa. Bishara hii imetimia sawasawa.

سُوْرَةُ الطَّارِقِ مَكِّيَّةٌ وَّ هِيَ مَعَ الْبَسْمَلَةِ ثَمَانِيَ عَشْرَةَ اٰيَةً وَّ رُكُوْعٌ

86. SURA AT-TAARIQ

Imeteremshwa Makka

Ina Aya 18 pamoja na Bismillahi

بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ ①

1. Kwa jina la Allah, Mwingi wa rehema, Mwingi wa ukarimu.

وَالسَّمَآءِ وَالطَّارِقِ ②

2. Naapa kwa mbingu na kwa kidhihirikacho usiku.

وَمَآ اَدْرٰىكَ مَا الطَّارِقُ ③

3. Na nini kitakujulisha kidhihirikacho usiku ni nini?

النَّجْمُ الثَّاقِبُ ④

4. Ni nyota ing'aayo sana.

اِنْ كُلُّ نَفْسٍ لَّمَّا عَلَيْهَا حَافِظٌ ⑤

5. Hakuna nafsi yo yote isiyo na mchungaji juu yake.

فَلْيَنْظُرِ الْاِنْسَانُ مِمَّ خُلِقَ ⑥

6. Basi mtu ajitazame ameumbwa kwa kitu gani,

خُلِقَ مِنْ مَّآءٍ دَافِقٍ ⑦

7. Ameumbwa kwa maji yaendayo kasi,

يَّخْرُجُ مِنْۢ بَيْنِ الصُّلْبِ وَالتَّرَآئِبِ ⑧

8. Yatokayo katikati ya mifupa ya mgongo na mbavu.

اِنَّهٗ عَلٰى رَجْعِهٖ لَقَادِرٌ ⑨

9. Kwa yakini Yeye Ana uwezo wa kumrudisha.

Sura hii ilishuka Makka. Baadhi ya marawi (wanaosimulia Hadithi za Mtume *s.a.w*) wanasema ya kwamba ilianguka nyota moja ya alfajiri, na Abu Jahal akaogopa, basi ndipo ziliposhuka Aya tatu za mwanzo wa sura hii.

Aya 2. *Taariq.* Neno hili lina maana tatu: (1) afikaye usiku; (2) Nyota ya alfajiri; (3) anayetupa changarawe kama makuhani wanaopiga falaki (Akrab).

Katika Aya ya 4 Allah Mwenyewe amekwisha onyesha ya kuwa muradi wa *Taariq* ni *Najmu thaaqib,* yaani nyota ing'aayo sana.

Aya 4. *Thaaqib,* "ing'aayo sana." Neno hili maana yake ni "atoboaye tundu." Ndiyo kusema *Najmu thaaqib* ni nyota itoboayo tundu katika giza, yaani inaliondoa (Akrab).

Aya 5. Watu wameifasiri Aya hii kwa maana mbalimbali. Allah ndiye Mlinzi wa kila mtu kama alivyosema katika Qur'an, *Allah ni Mlinzi wa kila kitu* (Ahzaab :3). Imesimuliwa na Mtume *s.a.w.* ya kuwa kila mwenye imani amewekewa Malaika 160 wanaomwondolea mawazo mabaya ya shetani kama wanavyoondolewa nzi ndani ya bakuli la asali (Ma'aani).

يَوْمَ تُبْلَى السَّرَآئِرُ ۙ﴿١٠﴾

10. Siku zitakapodhihirishwa siri,

فَمَا لَهٗ مِنْ قُوَّةٍ وَّلَا نَاصِرٍ ؕ﴿١١﴾

11. Basi hatakuwa na nguvu wala msaidizi.

وَالسَّمَآءِ ذَاتِ الرَّجْعِ ۙ﴿١٢﴾

12. Naapa kwa wingu lenye mvua kubwa,

وَالْاَرْضِ ذَاتِ الصَّدْعِ ۙ﴿١٣﴾

13. Na kwa ardhi inayopasuka (na kuotesha mimea);

اِنَّهٗ لَقَوْلٌ فَصْلٌ ۙ﴿١٤﴾

14. Kwa hakika hiyo ni kauli yenye uamuzi.

وَّمَا هُوَ بِالْهَزْلِ ؕ﴿١٥﴾

15. Wala hiyo si mzaha.

اِنَّهُمْ يَكِيْدُوْنَ كَيْدًا ۙ﴿١٦﴾

16. Hakika wao wanafanya hila,

وَّاَكِيْدُ كَيْدًا ۚ﴿١٧﴾

17. Nami pia nafanya mpango dhidi ya hila zao.

فَمَهِّلِ الْكٰفِرِيْنَ اَمْهِلْهُمْ رُوَيْدًا ۧ﴿١٨﴾

18. Basi wape makafiri muhula; wape muhula kwa muda fulani.

Aya 12. *Raj'a.* Neno hili lina muradi wa mvua inayokuja mara kwa mara (Akrab). Pia mvua imeitwa *raj'a* kwa sababu mawingu yake huzuka katika mvuke wa maji unaopanda kutoka baharini na kurejea kunyesha tena ardhini (Baidhawi).

سُوْرَةُ الْاَعْلٰى مَكِّيَّةٌ وَّ هِىَ مَعَ الْبَسْمَلَةِ عِشْرُوْنَ اٰيَةً وَّ رُكُوْعٌ

87. SURA AL-A'LAA

Imeteremshwa Makka

Ina Aya 20 pamoja na Bismillahi

بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ ①

1. Kwa jina la Allah, Mwingi wa rehema, Mwingi wa ukarimu.

سَبِّحِ اسْمَ رَبِّكَ الْاَعْلَى ②

2. Litukuze jina la Mola wako Aliye Mtukufu.

الَّذِىْ خَلَقَ فَسَوّٰى ③

3. Aliyeumba na Akastawisha.

وَالَّذِىْ قَدَّرَ فَهَدٰى ④

4. Na Aliyekadiria kisha Akaongoza.

وَالَّذِىْ اَخْرَجَ الْمَرْعٰى ⑤

5. Na Aliyechipusha malisho.

فَجَعَلَهٗ غُثَآءً اَحْوٰى ⑥

6. Halafu Akayafanya takataka nyeusi.

سَنُقْرِئُكَ فَلَا تَنْسٰٓى ⑦

7. Hivi karibuni Tutakusomesha wala hutasahau,

اِلَّا مَا شَآءَ اللّٰهُ ؕ اِنَّهٗ يَعْلَمُ الْجَهْرَ وَمَا يَخْفٰى ⑧

8. Ila Apendavyo Allah; Yeye Anajua yaliyo dhahiri na yaliyofichika.

وَنُيَسِّرُكَ لِلْيُسْرٰى ⑨

9. Nasi Tutakurahisishia yaliyo mepesi.

Karibu wanazuoni wote wanasema ya kuwa sura hii ilishuka Makka. Ibni Abbas, Ibni Zubair na Bibi Aisha pia wanasema kuwa sura hii ilishuka Makka. Imesimuliwa katika Musnad, Muslim na vitabu vingine vya Hadithi ya kuwa Nu'man bin Bashir alisema ya kuwa Mtume *s.a.w.* alikuwa anasoma sura hii katika rakaa ya kwanza ya Sala ya Ijumaa na rakaa za kwanza za Idi mbili. Seyidna Ali anasimulia ya kuwa Mtume *s.a.w.* alikuwa anaipenda sana sura hii (Musnad Ahmad).

Aya 7. *Wala hutasahau,* yaani mambo yote yaliyomo katika Qur'an hii Mtume hatayasahau. Ama kusahau ni tabia ya kila binadamu na Mtume pia alikuwa akisahau. Mathlan alisahau siku maalumu ya Lailat al Kadri alipokuwa akitoka kuwaambia watu; na pia alipata kusahau rakaa za Sala (Bukhari). Na pia Mtume *s.a.w.* alisema; "Ninasahau kama mnavyosahau ninyi" yaani katika mambo mengine ya kawaida.

Aya 9. Alipokuwa katika taabu za mji wa Makka, Allah akamwambia kuwa atamrahisishia mambo, na baadaye Mtume s.a.w. alipohamia Madina huko mambo yakawa rahisi kwake.

فَذَكِّرْ اِنْ نَّفَعَتِ الذِّكْرٰى ﴿١٠﴾

10. Basi utoe nasaha maana nasaha zina manufaa

سَيَذَّكَّرُ مَنْ يَّخْشٰى ﴿١١﴾

11. Bila shaka atashika nasaha mwenye kuogopa.

وَيَتَجَنَّبُهَا الْاَشْقَى ﴿١٢﴾

12. Na mwenye bahati mbaya atajitenga mbali nazo.

الَّذِىْ يَصْلَى النَّارَ الْكُبْرٰى ﴿١٣﴾

13. Ambaye atauingia Moto mkubwa.

ثُمَّ لَا يَمُوْتُ فِيْهَا وَلَا يَحْيٰى ﴿١٤﴾

14. Kisha humo hatakufa wala hatakuwa hai.

قَدْ اَفْلَحَ مَنْ تَزَكّٰى ﴿١٥﴾

15. Hakika amekwisha faulu aliyejitakasa,

وَذَكَرَ اسْمَ رَبِّهٖ فَصَلّٰى ﴿١٦﴾

16. Na akakumbuka jina la Mola wake na kusali.

بَلْ تُؤْثِرُوْنَ الْحَيٰوةَ الدُّنْيَا ﴿١٧﴾

17. Lakini ninyi mnayapenda zaidi maisha ya dunia,

وَالْاٰخِرَةُ خَيْرٌ وَّاَبْقٰى ﴿١٨﴾

18. Hali Akhera ni bora na yenye kudumu.

اِنَّ هٰذَا لَفِى الصُّحُفِ الْاُوْلٰى ﴿١٩﴾

19. Hakika haya yamo hata ndani ya misahafu iliyotangulia,

صُحُفِ اِبْرٰهِيْمَ وَمُوْسٰى ﴿٢٠﴾ ع

20. Misahafu ya Ibrahimu na Musa.

سُوْرَةُ الْغَاشِيَةِ مَكِّيَّةٌ وَّ هِيَ مَعَ الْبَسْمَلَةِ سَبْعٌ وَّ عِشْرُوْنَ اٰيَةً وَّ رُكُوْعٌ

88. SURA AL-GHAASHIYA

Imeteremshwa Makka

Ina Aya 27 pamoja na Bismillahi

بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ ①

1. Kwa jina la Allah, Mwingi wa rehema, Mwingi wa ukarimu.

هَلْ اَتٰىكَ حَدِيْثُ الْغَاشِيَةِ ②

2. Je! Imekuwasilia habari ya msiba unaofunikiza kabisa?

وُجُوْهٌ يَّوْمَئِذٍ خَاشِعَةٌ ③

3. Baadhi ya nyuso siku hiyo zitakuwa na hofu kubwa,

عَامِلَةٌ نَّاصِبَةٌ ④

4. (Kabla ya hapo, katika kuitafuta dunia) walikuwa ni wenye kujibidiisha mno na kuchoka sana.

تَصْلٰى نَارًا حَامِيَةً ⑤

5. Wataingia katika Moto uwakao.

تُسْقٰى مِنْ عَيْنٍ اٰنِيَةٍ ⑥

6. Watanyweshwa katika chemchem ichemkayo.

لَيْسَ لَهُمْ طَعَامٌ اِلَّا مِنْ ضَرِيْعٍ ⑦

7. Hawatakuwa na chakula isipokuwa cha miiba.

لَّا يُسْمِنُ وَلَا يُغْنِيْ مِنْ جُوْعٍ ⑧

8. Hakinenepeshi wala hakiondoi njaa.

وُجُوْهٌ يَّوْمَئِذٍ نَّاعِمَةٌ ⑨

9. Baadhi ya nyuso siku hiyo zitakuwa zenye kuchangamka.

Sura hii ilishuka Makka, na hakuna hitilafu juu ya jambo hili. Abdullah bin Abbas na Abdullah bin Zubair, wote wawili wanasimulia ya kwamba sura hii ilishuka Makka. Imesimuliwa na Nu'man bin Bashir katika Musnad Ibn Hanbal na Muslim na Sunani Nasai na Abu Dawud na Ibn Majah ya kuwa Mtume s.a.w. alikuwa anasoma katika rakaa ya kwanza ya Sala ya Ijumaa na Sala za Idi mbili sura A'laa na katika rakaa za pili sura hii Al-Ghaashiya. Hata kama Sala ya Ijumaa na ya Idi zilikutana katika siku moja, hata hivyo Mtume s.a.w. alikuwa anasoma sura hizi hizi katika sala zote mbili.

Aya 2. *Ghaashiyah,* "msiba unaofunikiza kabisa." Msiba huu ni wa siku ya Kiyama. Kadhalika makafiri wa Makka walifikiwa na msiba ambao unaonekana katika Aya hizi, nao ni wa njaa kubwa ya miaka saba ambayo Mtume *s.a.w.* aliomba akasema "Ee Mola wangu uwafikishie miaka saba kama ile ya Yusuf."

Aya 9. Hapa inaelezwa ya kuwa ingawa Waislamu katika Makka walikuwa na taabu, lakini siku zinakuja watakapokuwa na raha na makafiri watakuwa na dhiki.

لِّسَعْيِهَا رَاضِيَةٌ ﴿١٠﴾

10. Watakuwa wenye furaha sana kutokana na juhudi zao.

فِيْ جَنَّةٍ عَالِيَةٍ ﴿١١﴾

11. Katika Bustani iliyoinuka.

لَّا تَسْمَعُ فِيْهَا لَاغِيَةً ﴿١٢﴾

12. Hutasikia humo yasiyo na maana.

فِيْهَا عَيْنٌ جَارِيَةٌ ﴿١٣﴾

13. Humo chemchem inatiririka.

فِيْهَا سُرُرٌ مَّرْفُوْعَةٌ ﴿١٤﴾

14. Humo mna viti vya fahari vilivyoinuka.

وَّاَكْوَابٌ مَّوْضُوْعَةٌ ﴿١٥﴾

15. Na vikombe vilivyowekwa kwa utaratibu.

وَّنَمَارِقُ مَصْفُوْفَةٌ ﴿١٦﴾

16. Na matakia yaliyopangwa safu.

وَّزَرَابِيُّ مَبْثُوْثَةٌ ﴿١٧﴾

17. Na mazulia yaliyotandazwa.

اَفَلَا يَنْظُرُوْنَ اِلَى الْاِبِلِ كَيْفَ خُلِقَتْ ﴿١٨﴾

18. Je! hawatazami ngamia jinsi walivyoumbwa.

وَاِلَى السَّمَآءِ كَيْفَ رُفِعَتْ ﴿١٩﴾

19. Na mbingu jinsi ilivyoinuliwa.

وَاِلَى الْجِبَالِ كَيْفَ نُصِبَتْ ﴿٢٠﴾

20. Na milima jinsi ilivyosimikwa.

وَاِلَى الْاَرْضِ كَيْفَ سُطِحَتْ ﴿٢١﴾

21. Na ardhi jinsi ilivyotandazwa?

فَذَكِّرْ ؕ اِنَّمَاۤ اَنْتَ مُذَكِّرٌ ؕ ﴿٢٢﴾

22. Basi toa sana nasaha, hakika wewe ni mtoaji tu wa nasaha mara kwa mara.

لَسْتَ عَلَيْهِمْ بِمُصَيْطِرٍ ﴿٢٣﴾

23. Wewe si mlinzi wao.

اِلَّا مَنْ تَوَلّٰى وَكَفَرَ ﴿٢٤﴾

24. Ila anayerudi nyuma na kukataa.

فَيُعَذِّبُهُ اللّٰهُ الْعَذَابَ الْاَكْبَرَ ؕ ﴿٢٥﴾

25. Allah Atamwadhibu adhabu iliyo kubwa.

اِنَّ اِلَيْنَاۤ اِيَابَهُمْ ﴿٢٦﴾

26. Hakika marejeo yao ni Kwetu.

ثُمَّ اِنَّ عَلَيْنَا حِسَابَهُمْ ﴿٢٧﴾

27. Kisha bila shaka hesabu yao ni juu Yetu.

سُوْرَةُ الْفَجْرِ مَكِّيَّةٌ وَّ هِيَ مَعَ الْبَسْمَلَةِ اِحْدٰى وَ ثَلَا ثُوْنَ اٰيَةً وَّ رُكُوْعٌ

89. SURA AL-FAJR

Imeteremshwa Makka

Ina Aya 31 pamoja na Bismillahi

بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ ﴿١﴾

1. Kwa jina la Allah, Mwingi wa rehema, Mwingi wa ukarimu.

وَالْفَجْرِ ﴿٢﴾

2. Naapa kwa alfajiri,

وَلَيَالٍ عَشْرٍ ﴿٣﴾

3. Na kwa mausiku kumi,

وَّالشَّفْعِ وَالْوَتْرِ ﴿٤﴾

4. Na kwa shufwa na kwa witri,

وَالَّيْلِ اِذَا يَسْرِ ﴿٥﴾

5. Na kwa usiku upitapo.

هَلْ فِيْ ذٰلِكَ قَسَمٌ لِّذِيْ حِجْرٍ ﴿٦﴾

6. Je humo mna kiapo chochote kwa mwenye akili?

اَلَمْ تَرَ كَيْفَ فَعَلَ رَبُّكَ بِعَادٍ ﴿٧﴾

7. Je! Hukuona jinsi Mola wako Alivyowafanyia Waadi,

اِرَمَ ذَاتِ الْعِمَادِ ﴿٨﴾

8. Wairam (yaani waliotokana na Waadi, waliokuwa) wenye nguzo ndefu ndefu,

الَّتِيْ لَمْ يُخْلَقْ مِثْلُهَا فِي الْبِلَادِ ﴿٩﴾

9. Ujenzi wa namna ambayo haukuwahi kujengwa kabisa katika nchi zote;

وَثَمُوْدَ الَّذِيْنَ جَابُوا الصَّخْرَ بِالْوَادِ ﴿١٠﴾

10. Na Wathamudi waliochonga miamba katika bonde,

وَفِرْعَوْنَ ذِي الْاَوْتَادِ ﴿١١﴾

11. Na Firauni mwenye majeshi,

Sura hii pia ilishuka Makka. Mtungaji wa Tafsiri Fat'hul Bayan ameandika ya kuwa sura hii ni ya Makka bila hitilafu yo yote mbele ya wanazuoni. Ibni Abbas, Ibni Zubair na Bibi Aisha wote wanasema hivyo. Sura hii ilishuka katika majira ya kwanza ya Mtume kuwa Makka.

Aya 4. *Shufwa* na *Witri.* Shufwa ni tarakimu au idadi inayogawanywa kwa mbili na ikagawanyika bila kubaki, kama 2, 4, 6, 8, 10 n.k.w. Na witri ni hesabu au idadi iliyo kinyume na hiyo, kama 3, 5, 7, 9, 11 n.k.w. ambazo hazitagawanyika kwa mbili ila moja itabaki.

Aya 8. *Wairam.* Iram ni jina la babu ya 'Ad. Wengine wanasema Iram ni jina la mji walimokaa kabila la 'Ad (Razi).

الَّذِيْنَ طَغَوْا فِي الْبِلَادِ ﴿١٢﴾

12. Hawa ndio wale waliofanya uasi katika nchi mbali mbali;

فَاَكْثَرُوْا فِيْهَا الْفَسَادَ ﴿١٣﴾

13. Kisha walizidisha humo ufisadi?

فَصَبَّ عَلَيْهِمْ رَبُّكَ سَوْطَ عَذَابٍ ﴿١٤﴾

14. Kwa hiyo Mola wako Aliwapiga mjeledi wa adhabu.

اِنَّ رَبَّكَ لَبِالْمِرْصَادِ ﴿١٥﴾

15. Hakika Mola wako ni Mwenye kuvizia.

فَاَمَّا الْاِنْسَانُ اِذَا مَا ابْتَلٰىهُ رَبُّهٗ فَاَكْرَمَهٗ وَنَعَّمَهٗ ۙ فَيَقُوْلُ رَبِّيْٓ اَكْرَمَنِ ﴿١٦﴾

16. Ama mwanadamu, Mola wake Anapomjaribu na Akamtukuza na kumneemesha, basi husema: Mola wangu Amenitukuza.

وَاَمَّآ اِذَا مَا ابْتَلٰىهُ فَقَدَرَ عَلَيْهِ رِزْقَهٗ ۙ فَيَقُوْلُ رَبِّيْٓ اَهَانَنِ ﴿١٧﴾

17. Na ama Anapomjaribu na kumpunguzia riziki yake, husema: Mola wangu Amenidhalilisha.

كَلَّا بَلْ لَّا تُكْرِمُوْنَ الْيَتِيْمَ ﴿١٨﴾

18. Siyo! Bali ninyi hamuwaheshimu mayatima,

وَلَا تَحٰٓضُّوْنَ عَلٰى طَعَامِ الْمِسْكِيْنِ ﴿١٩﴾

19. Wala ninyi hamhimizi juu ya kuwalisha maskini.

وَتَاْكُلُوْنَ التُّرَاثَ اَكْلًا لَّمًّا ﴿٢٠﴾

20. Nanyi mnakula urithi kwa ulaji wa pupa,

وَّتُحِبُّوْنَ الْمَالَ حُبًّا جَمًّا ﴿٢١﴾

21. Na ninyi mnapenda mali kwa pendo la kupita kiasi.

كَلَّآ اِذَا دُكَّتِ الْاَرْضُ دَكًّا دَكًّا ﴿٢٢﴾

22. Sivyo! Itakapopondwa ardhi tikitiki,

وَّجَآءَ رَبُّكَ وَالْمَلَكُ صَفًّا صَفًّا ﴿٢٣﴾

23. Na Atafika Mola wako na Malaika safu-safu,

وَجِايْٓءَ يَوْمَئِذٍ بِجَهَنَّمَ ۙ يَوْمَئِذٍ يَّتَذَكَّرُ الْاِنْسَانُ وَاَنّٰى لَهُ الذِّكْرٰى ﴿٢٤﴾

24. Na Siku hiyo italetwa Jahanamu. Siku hiyo mwanadamu atatamani ashike nasaha, lakini sasa atawezaje kushika nasaha?

Aya 18. Yatima hapa ama ni Mtume s.a.w. au ni mtu ye yote aliye yatima. Mtume *s.a.w.* alisema, "Nyumba nzuri ni ile anamoheshimiwa yatima, na nyumba mbaya ni ile anamoudhiwa yatima."

Aya 19. Angalieni jinsi Islam ilivyokuwa na hamu ya kuwainua maskini.

يَقُوْلُ يٰلَيْتَنِيْ قَدَّمْتُ لِحَيَاتِيْ ﴿٢٥﴾

25. Atasema: Laiti ningalitanguliza (chochote) kwa ajili ya uhai wangu!

فَيَوْمَئِذٍ لَّا يُعَذِّبُ عَذَابَهٗٓ اَحَدٌ ﴿٢٦﴾

26. Basi Siku hiyo hataadhibu ye yote namna ya kuadhibu Kwake.

وَّلَا يُوْثِقُ وَثَاقَهٗٓ اَحَدٌ ﴿٢٧﴾

27. Wala hatafunga kibwebwe ye yote jinsi ya kufunga Kwake.

يٰٓاَيَّتُهَا النَّفْسُ الْمُطْمَئِنَّةُ ﴿٢٨﴾

28. Ewe roho uliyepata utulivu!

ارْجِعِيْٓ اِلٰى رَبِّكِ رَاضِيَةً مَّرْضِيَّةً ﴿٢٩﴾

29. Rudi kwa Mola wako hali ya kuridhika na kumridhisha.

فَادْخُلِيْ فِيْ عِبٰدِيْ ﴿٣٠﴾

30. Basi ingia katika watumishi wangu,

وَادْخُلِيْ جَنَّتِيْ ﴿٣١﴾ ع

31. Na ingia katika Pepo Yangu.

سُوْرَةُ الْبَلَدِ مَكِّيَّةٌ وَّ هِيَ مَعَ الْبَسْمَلَةِ اِحْدٰى وَ عِشْرُوْنَ اٰيَةً وَّ رُكُوْعٌ

90. SURA AL-BALAD

Imeteremshwa Makka

Ina Aya 21 pamoja na Bismillahi

بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ ①

1. Kwa jina la Allah, Mwingi wa rehema, Mwingi wa ukarimu.

لَآ اُقْسِمُ بِهٰذَا الْبَلَدِ ۙ ②

2. Zingatia, Naapa kwa mji huu.

وَاَنْتَ حِلٌّۢ بِهٰذَا الْبَلَدِ ۙ ③

3. Nawe utashuka katika mji huu.

وَوَالِدٍ وَّمَا وَلَدَ ۙ ④

4. Naapa kwa (baba) mzazi na kwa (mwanawe) aliyemzaa.

لَقَدْ خَلَقْنَا الْاِنْسَانَ فِيْ كَبَدٍ ؕ ⑤

5. Hakika Tulimwumba mtu adumu (kuishi) katika juhudi.

اَيَحْسَبُ اَنْ لَّنْ يَّقْدِرَ عَلَيْهِ اَحَدٌ ۘ ⑥

6. Je! anadhani ya kuwa hapana ye yote mwenye uwezo juu yake?

يَقُوْلُ اَهْلَكْتُ مَالًا لُّبَدًا ؕ ⑦

7. Anasema: Nimeharibu mali nyingi (bure).

اَيَحْسَبُ اَنْ لَّمْ يَرَهٗۤ اَحَدٌ ؕ ⑧

8. Je! anadhani ya kuwa hapana ye yote amwonaye?

اَلَمْ نَجْعَلْ لَّهٗ عَيْنَيْنِ ۙ ⑨

9. Je! Hatukumpa macho mawili,

وَلِسَانًا وَّشَفَتَيْنِ ۙ ⑩

10. Na ulimi, na midomo miwili,

وَهَدَيْنٰهُ النَّجْدَيْنِ ۚ ⑪

11. Na Tukamwonyesha njia mbili zilizoinuka?

Ibni Abbas na Ibni Zubair wanaeleza ya kuwa sura hii ilishuka Makka, mwishoni mwa mwaka wa tatu au mwanzoni mwa mwaka wa nne wa utume.

Aya 3. Hapa Mtume *s.a.w.* anaahidiwa ya kwamba ataingia katika mji wa Makka katika hali ya adhma na ushindi, na yote hii atapata kwa sababu ya taabu na mashaka aliyobeba zamani.

Aya 11. *Njia mbili zilizoinuka* ni njia za maendeleo ya dunia na ya dini, au ni njia za wema na ubaya.

فَلَا اقْتَحَمَ الْعَقَبَةَ ﴿١٢﴾

12. Lakini hakufuata njia ya 'Aqabah'.

وَمَآ اَدْرٰىكَ مَا الْعَقَبَةُ ﴿١٣﴾

13. Na nini kitakujulisha njia ya 'Aqabah' ni nini?

فَكُّ رَقَبَةٍ ﴿١٤﴾

14. Ni kumpa mtumwa uungwana,

اَوْ اِطْعٰمٌ فِيْ يَوْمٍ ذِيْ مَسْغَبَةٍ ﴿١٥﴾

15. Au kumlisha siku ya njaa,

يَّتِيْمًا ذَا مَقْرَبَةٍ ﴿١٦﴾

16. Yatima jamaa,

اَوْ مِسْكِيْنًا ذَا مَتْرَبَةٍ ﴿١٧﴾

17. Au maskini hohe hahe.

ثُمَّ كَانَ مِنَ الَّذِيْنَ اٰمَنُوْا وَتَوَاصَوْا بِالصَّبْرِ وَتَوَاصَوْا بِالْمَرْحَمَةِ ﴿١٨﴾

18. Kisha awe miongoni mwa waaminio na wanaousiana kusubiri na wanaousiana kuhurimiana.

اُولٰٓئِكَ اَصْحٰبُ الْمَيْمَنَةِ ﴿١٩﴾

19. Hao ndio watu wa upande wa kuume.

وَالَّذِيْنَ كَفَرُوْا بِاٰيٰتِنَا هُمْ اَصْحٰبُ الْمَشْئَمَةِ ﴿٢٠﴾

20. Lakini waliozikataa Aya Zetu, hao ndio watu wa upande wa kushoto;

عَلَيْهِمْ نَارٌ مُّؤْصَدَةٌ ﴿٢١﴾

21. Moto uliofunikwa utakuwa juu yao.

Aya 12. *Njia ya mlimani,* ni njia imfikishayo mtu kwenye wema hasa.

سُوْرَةُ الشَّمْسِ مَكِّيَّةٌ وَّ هِيَ مَعَ الْبَسْمَلَةِ سِتَّ عَشْرَةَ اٰيَةً وَّ رُكُوْعٌ

91. SURA ASH-SHAMS

Imeteremshwa Makka

I*na Aya 16 pamoja na Bismillahi*

بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ ①

1. Kwa jina la Allah, Mwingi wa rehema, Mwingi wa ukarimu.

وَالشَّمْسِ وَضُحٰهَا ۙ ②

2. Naapa kwa jua na kwa mwanga wake,

وَالْقَمَرِ اِذَا تَلٰهَا ۙ ③

3. Na kwa mwezi unapoliandama,

وَالنَّهَارِ اِذَا جَلّٰهَا ۙ ④

4. Na kwa mchana unapolidhihirisha,

وَالَّيْلِ اِذَا يَغْشٰهَا ۙ ⑤

5. Na kwa usiku unapolifunika,

وَالسَّمَآءِ وَمَا بَنٰهَا ۙ ⑥

6. Na kwa mbingu na kwa namna Alivyoitengeneza.

وَالْاَرْضِ وَمَا طَحٰهَا ۙ ⑦

7. Na kwa ardhi na kwa namna Alivyoitandaza,

وَنَفْسٍ وَّمَا سَوّٰىهَا ۙ ⑧

8. Na kwa kila nafsi na kwa jinsi Alivyoistawisha vizuri,

فَاَلْهَمَهَا فُجُوْرَهَا وَتَقْوٰىهَا ۙ ⑨

9. Kisha Akaifunulia maovu yake na wema wake;

قَدْ اَفْلَحَ مَنْ زَكّٰىهَا ۙ ⑩

10. Bila shaka amefaulu aliyeitakasa;

Sura hii ilishuka Makka. Ibni Abbas anasimulia ya kuwa ilishuka Makka. Ukba bin Aamir anasimulia ya kwamba Mtume s.a.w. aliwaamrisha watu kusoma sura Shams na sura Dhuha katika Sala ya Adhuhuri (Fat'hul Bayan).

Aya 2. *Naapa kwa jua.* Muradi wa jua hapa ni Mtume Muhammad *s.a.w.*

Aya 3. *Na kwa mwezi.* Mwezi ni sayari inayochukua nuru yake toka kwa jua, na hapa muradi wake ni Masihi Aliyeahidiwa, au watu watawa watakaochukua nuru ya Mtume *s.a.w.* na kuizagaza duniani kama vile mwezi unavyoonyesha nuru ya jua.

Aya 10. *Amefaulu aliyeitakasa.* Yaani aliyeitakasa nafsi yake kwa kufuata nuru ya Mtume Muhammad *s.a.w.* Kama watu wanatakasa nafsi zao na kusafisha roho zao, bila shaka hao ndio

وَقَدْ خَابَ مَنْ دَسّٰىهَا ﴿١١﴾

11. Na bila shaka amejihasiri aliyeifukia.

كَذَّبَتْ ثَمُوْدُ بِطَغْوٰىهَآ ﴿١٢﴾

12. Wathamudi walikadhibisha kutokana na uasi wao mkubwa.

اِذِ انْۢبَعَثَ اَشْقٰىهَا ﴿١٣﴾

13. Aliposimama mwovu wao mkubwa.

فَقَالَ لَهُمْ رَسُوْلُ اللّٰهِ نَاقَةَ اللّٰهِ وَسُقْيٰهَا ﴿١٤﴾

14. Hapo Mtume wa Allah akawaambia: (Huyu) ni ngamia wa Allah, (na mzingatie) haki yake ya kunywa maji.

فَكَذَّبُوْهُ فَعَقَرُوْهَا ۖ فَدَمْدَمَ عَلَيْهِمْ رَبُّهُمْ بِذَنْۢبِهِمْ فَسَوّٰىهَا ﴿١٥﴾

15. Lakini walimkadhibisha na wakaikata miguu yake, kwa hiyo Mola wao Aliwaangamiza kwa sababu ya dhambi zao, na Akawafuta kabisa.

وَلَا يَخَافُ عُقْبٰهَا ﴿١٦﴾

16. Wala Haogopi matokeo yake.

---

wanaopata ufaulu. Lakini asiyetakasa nafsi yake katika nuru ya Mtume *s.a.w.* yeye kwa hakika anadidimiza nafsi yake katika uchafu, na hivyo anashindwa na anapata hasara, maana kwa kuacha nuru na kukaa katika giza, anawezaje kupata ufaulu?

Aya 16. *Wala Haogopi matokeo yake.* Watu wa kabila la Thamudi walishindana na Nabii wao wakaangamizwa, na kadhalika makafiri wa Makka wakashindana na Mtume *s.a.w.* katika kazi zake. Hivyo wanaonywa ya kuwa nao wataangamizwa vile vile, na Allah hatajali kabisa matokeo yatakayojiri.

سُوْرَةُ الَّيْلِ مَكِّيَّةٌ وَّ هِيَ مَعَ الْبَسْمَلَةِ اثْنَتَانِ وَ عِشْرُوْنَ اٰيَةً وَّ رُكُوْعٌ

92. SURA AL-LAIL

Imeteremshwa Makka

Ina Aya 22 pamoja na Bismillahi

بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ ①

1. Kwa jina la Allah, Mwingi wa rehema, Mwingi wa ukarimu.

وَالَّيْلِ اِذَا يَغْشٰى ۙ ②

2. Naapa kwa usiku ufunikapo,

وَالنَّهَارِ اِذَا تَجَلّٰى ۙ ③

3. Na kwa mchana uangazapo,

وَمَا خَلَقَ الذَّكَرَ وَالْاُنْثٰى ۙ ④

4. Na kwa Yule Aliyeumba kiume na kike.

اِنَّ سَعْيَكُمْ لَشَتّٰى ؕ ⑤

5. Hakika bidii yenu ni mbalimbali.

فَاَمَّا مَنْ اَعْطٰى وَاتَّقٰى ۙ ⑥

6. Lakini anayetoa (katika njia ya Allah) na kumcha (Allah),

وَصَدَّقَ بِالْحُسْنٰى ۙ ⑦

7. Na kulisadikisha jambo jema kabisa,

فَسَنُيَسِّرُهٗ لِلْيُسْرٰى ؕ ⑧

8. Basi Tutamrahisishia mambo kuwa mepesi.

وَاَمَّا مَنْۢ بَخِلَ وَاسْتَغْنٰى ۙ ⑨

9. Na kuhusiana na yule aliyefanya ubakhili na kudhihirisha kutokujali,

وَكَذَّبَ بِالْحُسْنٰى ۙ ⑩

10. Na kukadhibisha jambo jema,

فَسَنُيَسِّرُهٗ لِلْعُسْرٰى ؕ ⑪

11. Basi tutamrahisishia kupata taabu.

وَمَا يُغْنِىْ عَنْهُ مَالُهٗۤ اِذَا تَرَدّٰى ؕ ⑫

12. Na mali yake itakapoangamia, haitamfaa chochote.

Kwa kauli ya wanazuoni wote sura hii ilishuka Makka. Abdullah bin Abbas na Abdullah bin Zubair pia wanasema hivyo hivyo.

Aya 6. Mtu anayetoa sadaka katika njia za dini na kufuata haki yeye hupata raha duniani na Akhera.

13. Hakika kuongoza ni juu Yetu. إِنَّ عَلَيْنَا لَلْهُدٰى ﴿١٣﴾

14. Na bila shaka mwisho upo ndani ya uwezo wetu na mwanzo pia. وَإِنَّ لَنَا لَلْآخِرَةَ وَالْأُولٰى ﴿١٤﴾

15. Basi nawahadharisheni na Moto uwakao. فَأَنْذَرْتُكُمْ نَارًا تَلَظّٰى ﴿١٥﴾

16. Hatauingia ila mwenye bahati mbaya sana. لَا يَصْلٰهَا إِلَّا الْأَشْقَى ﴿١٦﴾

17. Aliyekadhibisha na kurudi nyuma. الَّذِي كَذَّبَ وَتَوَلّٰى ﴿١٧﴾

18. Na amchaye Allah ataepushwa nao, وَسَيُجَنَّبُهَا الْأَتْقَى ﴿١٨﴾

19. Ambaye hutoa mali yake kujitakasa. الَّذِي يُؤْتِي مَالَهُ يَتَزَكّٰى ﴿١٩﴾

20. Na hapana ye yote aliyemfanyia hisani ili apate kulipwa, وَمَا لِأَحَدٍ عِنْدَهُ مِنْ نِعْمَةٍ تُجْزٰى ﴿٢٠﴾

21. Isipokuwa kupata radhi ya Mola Wake Aliye juu. إِلَّا ابْتِغَاءَ وَجْهِ رَبِّهِ الْأَعْلٰى ﴿٢١﴾

22. Naye hivi karibuni atakuwa radhi ع ١٧ وَلَسَوْفَ يَرْضٰى ﴿٢١﴾

Aya 19. Ingawa masahaba wote walikuwa wanafanya bidii sana kutoa mali zao katika njia ya dini, lakini Seyidna Abu Bakar alizidi, hata Mtume *s.a.w.* akasema, "Haiukunifaa mali ya mtu ye yote kamwe kama ilivyonifaa mali ya Abu Bakar" (Tirmidhi).

سُوْرَةُ الضُّحٰى مَكِّيَّةٌ وَّ هِىَ مَعَ الْبَسْمَلَةِ اثْنَتَا عَشْرَةَ اٰيَةً وَّ رُكُوْعٌ

93. SURA ADH-DHUHAA

Imeteremshwa Makka

Ina Aya 12 pamoja na Bismillahi

بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ ①

1. Kwa jina la Allah, Mwingi wa rehema, Mwingi wa ukarimu.

وَالضُّحٰى ②

2. Naapa kwa mchana,

وَالَّيْلِ اِذَا سَجٰى ③

3. Na kwa usiku unapotanda.

مَا وَدَّعَكَ رَبُّكَ وَمَا قَلٰى ④

4. Hakukuacha Mola wako wala Hakukukasirikia.

وَلَلْاٰخِرَةُ خَيْرٌ لَّكَ مِنَ الْاُوْلٰى ⑤

5. Na bila shaka wakati ujao ni bora kwako kuliko uliotangulia.

Ibni Abbas anasimulia ya kuwa sura hii ilishuka Makka. Ulikatika wahyi na sura hii baadaye ikashuka, Mtume *s.a.w.* alipokuwa anaisoma au kumsikia mtu anaisoma, aliamrisha watu wasome takbira, *Allahu Akbar* (Mungu ni Mkuu kabisa), na pengine alikuwa anasoma, *Allaahu akbar, Allahu akbar, la ilaaha illallaahu Allaahu akbar.*

Aya 2. *Ad-dhuhaa.* Neno hili maana yake ni wakati ule mchana unapoanza mpaka jua linapoanza kupinduka (Akrab).

Katika maisha yote ya Mtume *s.a.w.* mchana mmoja na usiku mmoja uliopata kumfikia ulikuwa wenye maana sana. Usiku ni ule aliondoka Makka kwa kuhamia Madina, na mchana ni ule aliofika Makka kutoka Madina, na mji wa Makka ukaangukia mikononi mwake. Usiku huu na mchana huu ni kitu chenye maana kubwa katika uhai wake, na Allah anatoa ushahidi wa mchana ule na usiku ule kuhakikisha ya kwamba hakumwacha Mtume *s.a.w.* wala hakumkasirikia.

Ndiyo kusema, Mtume *s.a.w.* usiku alipohama Makka nyumba yake ilikuwa imezungukwa na maadui waliokwenda kumwua. Ingekuwa Mungu Alimkasirikia asingeweza kupona na bila shaka angeangamia. Kadhalika alipokuja kuishinda Makka ilikuwa ni mchana kweupe, maadui zake wanaona na Mungu na Malaika wake pia wanamwona. Hivyo kama Mtume *s.a.w.* angekuwa amekasirikiwa na Allah asingeachwa ashinde na afanikiwe. Kwa neno zima usiku ule na mchana ule vinahakikisha kuwa Mungu alikuwa pamoja na Mtume *s.a.w.*

Aya 4. Katika siku za mwanzo za utume, wahyi haukuja kwa Mtume *s.a.w.* kwa siku mbili tatu. Dada wa Abu Sufyan akamwambia Mtume *s.a.w.* ya kuwa "Shetani wako amekuacha." Mtume *s.a.w.* akahuzunika sana. Basi Allah akateremsha Aya hii kumfariji na kumwambia kuwa kila wakati wako ujao unakuwa bora zaidi kuliko uliopita, na utaendelea namna hii kuzidishiwa heri. Basi Mungu Hakukuacha bali Anakusaidia.

وَلَسَوْفَ يُعْطِيكَ رَبُّكَ فَتَرْضٰى ۝٦

6. Na Mola wako hivi karibuni Atakupa na utaridhika.

اَلَمْ يَجِدْكَ يَتِيْمًا فَاٰوٰى ۝٧

7. Je! Hakukukuta u yatima na Amekupa makao?

وَوَجَدَكَ ضَآلًّا فَهَدٰى ۝٨

8. Na Akakukuta ukihangaika (kuongoza watu) naye Amekuongoza?

وَوَجَدَكَ عَآئِلًا فَاَغْنٰى ۝٩

9. Na Akakukuta mhitaji naye Amekutajirisha?

فَاَمَّا الْيَتِيْمَ فَلَا تَقْهَرْ ۝١٠

10. Basi usimkemee yatima,

وَاَمَّا السَّآئِلَ فَلَا تَنْهَرْ ۝١١

11. Wala usimkaripie aombaye.

وَاَمَّا بِنِعْمَةِ رَبِّكَ فَحَدِّثْ ۝١٢ ع ١١

12. Na ama neema za Mola wako, basi uzisimulie kwa wingi.

Aya 7. *Hakukukuta yatima?* Abdullah, baba wa Mtume *s.a.w.* alifariki dunia miezi mitatu kabla Mtume hajazaliwa; mama yake, Amina akafariki Mtume alipokuwa na umri wa miaka sita, na babu yake, Abdul Muttalib, aliyemchukua kumlea akafa Mtume alipokuwa na umri wa mika minane. Basi namna hii Mtume alibaki yatima kabisa na alilelewa na baba yake mdogo, aitwaye Abu Talib.

Aya 8. *Dhaallan.* Neno hili mapadre wamelifasiri "kupotea" katika shauku yao ya kutaka kuonyesha kuwa Mtume s.a.w. alikuwa na dhambi. Wanatafsiri Aya hii hivi; Hakukukuta umepotea njia akakuongoza?' (Padre Dale). Lakini neno *dhaallan* hapa halina maana ya "kupotea njia" wala si siku zote katika Kiarabu linapokuwa na maana hiyo. Neno hilo limetafsiriwa na Allah Mwenyewe katika sura hii hii. Mtume alikutwa na shida tatu na akazitimiziwa na akaambiwa maagizo matatu: (1) Alikutwa yatima, Mungu anamwambia, "Usimkaripie yatima" (Aya ya 10). (2) Alikutwa dhaallan (Ahangaikaye na aombaye radhi ya Mungu). Mungu anamwambia, "Wala usimkaripiye aombaye" (Aya ya 11). (3) Alikuwa mhitaji, Mungu anamwambia, "Dhihirisha neema za Mola wako ulizopewa. Hivyo hakuna hapa habari za kupotea. Isitoshe historia inahakikisha ya kuwa Mtume toka utoto wake alikuwa akichukia sana masanamu, na hakupata kusema uwongo hata mara moja, wala hakuwa akitoka kwenda cheza na wenziwe. Na alijulikana kuwa mwaminifu kabisa. Hivyo maneno haya ya mapadre si ya kweli, bali ni ya uadui tu.

سُوْرَةُ اَلَمْ نَشْرَحْ مَكِّيَّةٌ وَّ هِيَ مَعَ الْبَسْمَلَةِ تِسْعُ اٰيَاتٍ وَّ رُكُوْعٌ

94. SURA ALAM NASHRAH

Imeteremshwa Makka

Ina Aya 9 pamoja na Bismillahi

بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ ①

1. Kwa jina la Allah, Mwingi wa rehema, Mwingi wa ukarimu.

اَلَمْ نَشْرَحْ لَكَ صَدْرَكَ ۙ ②

2. Je! Hatukukupanulia kifua chako?

وَوَضَعْنَا عَنْكَ وِزْرَكَ ۙ ③

3. Na Tumekuondolea mzigo wako,

الَّذِيْٓ اَنْقَضَ ظَهْرَكَ ۙ ④

4. Uliokulemea mgongo wako,

وَرَفَعْنَا لَكَ ذِكْرَكَ ؕ ⑤

5. Na Tukakunyanyulia sifa zako?

فَاِنَّ مَعَ الْعُسْرِ يُسْرًا ۙ ⑥

6. Basi kwa hakika pamoja na dhiki iko faraja.

اِنَّ مَعَ الْعُسْرِ يُسْرًا ؕ ⑦

7. Hakika pamoja na dhiki iko faraja.

فَاِذَا فَرَغْتَ فَانْصَبْ ۙ ⑧

8. Basi upatapo faragha fanya juhudi.

وَاِلٰى رَبِّكَ فَارْغَبْ ۧ ⑨

9. Na kwa Mola wako elekea kwa shauku.

Sura hii ilishuka Makka na hakuna hitilafu (Fat'hul Bayan). Inaonekana ya kuwa sura hii ilishuka mwaka wa tatu au karibu yake baada ya Mtume *s.a.w.* kupata utume.

Aya 2. Kilipanuliwa kwa nuru ya kiungu na utulivu uliotoka kwa Allah na kwa ufunuo na Malaika kumsaidia (Mufradat).

Aya 4. Mzigo aliopewa Mtume *s.a.w.* ni mkubwa kabisa. Kuwafikishia watu wa dunia nzima ujumbe na kuwaingiza katika Uislamu, kuwasuluhisha na kuwaachisha mila zao mbaya na kuwaachisha dini za uwongo, hakika huu ni mzigo mkubwa, na yeye ni peke yake. Huu ndio mzigo uliomwelemea Mtume *s.a.w.* na Allah akamfanyia kazi yake kuwa rahisi.

سُوْرَةُ التِّيْنِ مَكِّيَّةٌ وَّ هِيَ مَعَ الْبَسْمَلَةِ تِسْعُ اٰيَاتٍ وَّ رُكُوْعٌ

95. SURA AT-TIIN

Imeteremshwa Makka

Ina Aya 9 pamoja na Bismillahi

بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ ①

1. Kwa jina la Allah, Mwingi wa rehema, Mwingi wa ukarimu.

وَالتِّيْنِ وَالزَّيْتُوْنِ ②

2. Naapa kwa Tini na Zeituni,

وَطُوْرِ سِيْنِيْنَ ③

3. Na kwa mlima Sinai,

وَهٰذَا الْبَلَدِ الْاَمِيْنِ ④

4. Na kwa Mji huu wenye amani,

لَقَدْ خَلَقْنَا الْاِنْسَانَ فِيْٓ اَحْسَنِ تَقْوِيْمٍ ⑤

5. Bila shaka Tumemwumba mtu kwa rasimu iliyo bora kabisa miongoni mwa rasimu za uumbaji.

ثُمَّ رَدَدْنٰهُ اَسْفَلَ سٰفِلِيْنَ ⑥

6. Halafu Tukamrudisha katika hali ya chini kabisa kuliko ya wale walio chini,

اِلَّا الَّذِيْنَ اٰمَنُوْا وَعَمِلُوا الصّٰلِحٰتِ فَلَهُمْ اَجْرٌ غَيْرُ مَمْنُوْنٍ ⑦

7. Isipokuwa wale wenye kuamini na kutenda mema, basi watakuwa na ujira usiokwisha.

فَمَا يُكَذِّبُكَ بَعْدُ بِالدِّيْنِ ⑧

8. Basi baada yake kuna nini kitakachokukadhibisha katika dini?

اَلَيْسَ اللّٰهُ بِاَحْكَمِ الْحٰكِمِيْنَ ⑨

9. Je! Allah si Hakimu Mbora kuliko mahakimu wote?

Ibni Abbas na Ibn Zubair wanasema ya kuwa sura hii ilishuka Makka, na wanazuoni wote wanakubali jambo hili.

Aya 2. Neno la Tin linaashiria kwa Nabii Adamu (Mwanzo 3:1-7), Zeituni linaashiria kwa Nabii Nuhu (Mwanzo 8:12). Mlima Sinai linaashiria kwa Nabii Musa, na mji huu wenye amani ni ishara kwa Mtume Muhammad s.a.w. ya kwamba Manabii hawa ni ushahidi wa kwamba Allah amemwumba mwanadamu kwa umbo bora.

Aya 5. *Tulimwumba mtu kwa umbo bora.* Aya hii inaonyesha ya kwamba asili ya mwanadamu ni bora, na dhambi ni kitu tu anachochuma mwenyewe, ambacho hakiko katika asili yake.

Fundisho hili ni hitilafu na fundisho la Kikristo linalosema kuwa kukosa kwa Adamu na Hawa ndiko kumeleta dhambi ya kwanza hapa duniani, na ya kwamba kila mtu anayezaliwa anazaliwa na dhambi hiyo. Wanasema ya kuwa Mungu hawezi kuwasamehe watu dhambi zao bure, mpaka itoke kafara, na kafara hiyo ni Yesu bin mariamu, mwana wa Mungu, aliyejitoa auawe ili achukue dhambi za watu nao waokoke.

Jambo hili ni katika misingi ya dini ya Kikristo. Hitilafu hii ni kubwa baina yetu sisi na wao. Sisi tunasadiki tunavyofundishwa na Qur'an na Mtume Muhammad *s.a.w*. ya kwamba Mungu ni Mwenye rehema na ni Mwenye kughofiri madhambi. Kila mtu na awe na dhambi nyingi zilizojaa dunia yote na mbingu yote, lakini mara akijitupa kwa Allah na kufanya toba ya kweli, asiwe na nia ya kurejea madhambi, bila shaka Mungu atamsamehe kabisa madhambi yake, wala hapana haja ya kuwa mtu mwingine ajitoe kuuawa kama kafara kwa ajili yake, na awe mtu mwema namna gani. Hivyo jambo hili tunalijadili kwa urefu kidogo:-

Wakristo wanasema ya kuwa Mungu alimweka Adamu na Hawa katika bustani. Akawaambia wale matunda ya miti yote isipokuwa mti wa "Kujua mema na Mabaya" m a a n a wakiula huo watakufa. Nyoka akamwendea Hawa, akamdanganya ya kwamba akilila tunda lile atakuwa naye sawa na Mungu, atajua mema na mabaya. Hawa akadanganyika, akalila, na akampelekea Adamu naye akala. Walipokwisha kula, Mungu akawaapiza nyoka, Hawa na Adamu.

Nyoka akaambiwa, "Umelaaniwa wewe kuliko wanyama wote, na kuliko kila mnyama wa bara; utatambaa kwa tumbo lako, nawe utakula mchanga siku zote za maisha yako: nami nitatia uadui kati ya wewe na huyo mwanamke, na kati ya uzao wako na uzao wake; huo utakusheta kichwa chako, na wewe utamsheta kisigino chake" (Mwanzo 3:14-15).

Hawa naye akaambiwa, Nitazidisha sana usumbufu wako na kutunga mimba kwako katika uchungu utazaa watoto, na tamaa yako itakuwa ikimwelemea mumeo, naye atatawala juu yako (Mwanzo 3:16).

Adamu naye akaambiwa, "Hii nchi imelaaniwa kwa ajili yako wewe; utakula viliwa vyake katika taabu siku zote za maisha yako; nayo itakumeeshea miiba na mibaruti-mwitu; nawe utakula majani ya mashamba; katika jasho la uso wako utakula chakula chako, hata utakaporejea katika udongo" (Mwanzo 3:17-19).

Wakristo wanatuambia ya kuwa wanadamu wote kila wanapozaliwa wanakuja duniani hali wamekwisha rithi dhambi hiyo ya Adamu. Sababu yake, wasemavyo Wakatoliki, ni kwamba mfalme akiondolewa katika ufalme, basi na wanawe pia wanakosa haki ya kutawala, au kama vile mtoto kurithi ugonjwa wa wazazi wake. Juu ya hayo bila kutoa sababu wanasema Mariamu mama wa Yesu hakurithi dhambi hiyo ya asili ingawa wazazi wake walikuwa nayo, na Yesu pia wanasema, hakurithi dhambi hiyo. Wanatuambia ya kuwa watu wanaobatizwa ndio huondokewa na dhambi ya asili, wakikiri kuwa Yesu ni mwokozi wao, ambaye amekufa msalabani kuwakomboa, naye amejitoa kuwa kafara, ili achukue dhambi za dunia nzima, na wanaomwamini wapone.

Wakatoliki na Waprotestanti wanapatana sana katika itikadi hii.

Sasa tuyahoji mafundisho hayo kidogo kidogo:-

1. Kosa tunaloambiwa alifanya Hawa na Adamu ni "kula mti wa kujua mema na mabaya." Ndiyo kusema kabla hawajaula mti ule walikuwa ni watu wasio na uwezo wa kupambanua wema ni nini na ubaya ni nini Yaani hawakuwa na ujuzi wa kibinadamu. Wangekuwa na ujuzi wa kupambanua wema na ubaya, kisha wakakosa, hapo wangelaumiwa, maana wamekosa hali ya kujua. Lakini Hawa na mumewe walikuwa hawajui lo lote. Na anayekosa kwa sababu amenyimwa uwezo wa kutambua, hastahili adhabu. Hivyo kuadhibiwa Hawa na Adamu juu ya jambo hili ni kuonewa bure.

2. Kusema ya kwamba kosa la Hawa na mumewe limeambukizwa wanadamu wote, na ya kwamba wanaadhibiwa kwa sababu ya kosa hili, bila shaka ni kuonewa. Kwanza hakuna mtu ye yote aliyemwambia Mungu kuwa azaliwe na Hawa na Adamu ambao wamekwisha kosa. Kuzaliwa kwao nao ni kushurutishwa tu. Na kama watashurutishwa pia kurithi dhambi yao, ili wapate

kuadhibiwa kwa kosa ambalo si lao, basi itakuwa kumshtaki Mungu kuwa anawaonea watu, hata kanuni za watu wenye akili hazimwadhibu mtoto kwa kosa la baba yake. Hata kama ni mfalme, kwa wenye akili aondolewapo baba yake kwa kosa, mtoto hutawalishwa. Wala siyo kila mara mtoto hurithi ugonjwa wa wazazi wake. Watu wenye maarifa hawaruhusu watoto wao kurithi magonjwa yao. Madaktari huweza kumtibu mama kabla hajazaa na mtoto akazaliwa hana ugonjwa wa mama yake. Je hao wote wana maarifa zaidi kuliko Mungu, hata ashindwe kumfanya mtoto wa wazazi wenye kosa kuzaliwa pasipo kosa?

3. Biblia yenyewe inatuonyesha majina ya watu wengi ambao walikuwa watukufu mbele ya Mungu, nao ni binadamu, watu ambao waliokoka bila kubatizwa kwa jina la Yesu. Kama ni kweli waliirithi dhambi ile, basi waliokoka namna gani? Kwa mfano tunasoma:-

(a) "Enok (Idrisa) alikuwa akienda pamoja na Allah: kisha asionekane; kwa kuwa Allah alimtwaa" (Mwanzo 5:24). Wakristo wanasadiki ya kuwa Enok alikwenda mbinguni na kiwiliwili chake. Inaonekana aliokoka. Adhabu mojawapo aliyopewa Adamu ni kufa na kuzikwa ardhini (Mwanzo 3:19). Lakini Wakristo wanasema Enok hakufa, alikwenda mbinguni. Ingekuwa kweli Adamu alifanya dhambi ya kurithiwa na watu, ilikuwaje Enok akatembea pamoja na Mungu, na kuchukuliwa naye mbinguni, hali Yesu na wafuasi wake walikuwa hawajajulikana kama watafika ardhini kuja batiza watu?

(b) Nuhu anasemwa, "Alikuwa ni mtu mwenye haki, mtimilifu katika vizazi vyake: Nuhu alikuwa akienda pamoja na Allah" (Mwanzo 6:9). Na Lamek babaye Nuhu, alipomzaa Nuhu akasema, "Huyo atatuliza nyoyo kwa ajili ya kazi yetu yote na kwa ajili ya taabu ya mikono yetu, kwa sababu ya hii nchi ambayo Jehova ameilaani" (Mwanzo 5:29). Imeandikwa ya kuwa Mungu alithubutisha agano lake na Nuhu (Mwanzo 6:18), "Nuhu akamjengea Jehova madhabahu: naye akatwaa kila mnyama aliyekuwa tohara, na kila ndege aliyekuwa tohara, akachinja sadaka za kuteketezwa juu ya madhabahu. Jehova akapata harufu, harufu ipendezayo: na Jehova akasema moyoni mwake, Sitailaani nchi tena kabisa kwa ajili ya bin-Adamu" (Mwanzo 8:20-21). Ni wazi kwa maneno haya ya kuwa Nuhu hakuwa na lawama mbele ya Mungu, hata Mungu akafurahi naye, na ile laana inayosemwa ililaaniwa nchi (Mwanzo 3:17) hapa imebatilishwa. Na Mungu anasema hatailaani tena nchi. Je kama ni kweli kosa la hawa na Adamu liliwagandama wanadamu wote, kwa nini kisa hiki cha Nuhu kinabatilisha fundisho hilo la Wakristo?

(c) Zakaria na mkewe "wote wawili wenye haki mbele za Mungu. wakiendelea katika amri zote za Bwana na hukumu zake zote bila lawama" (Luka 1:6).

(d) Nabii Yahya (Yohana) alibashiriwa na Malaika kuwa "atakuwa mkuu mbele ya Mungu, hatakunywa divai wala kileo; naye atajazwa roho Mtakatifu hata tangu tumbo la mama yake. Na wengi katika wana wa Israeli atawarejeza kwa Bwana Mungu wao" (Luka 1:15-16).

Hao wote walikuwa kabla ya Yesu na ni watu waliookoka. Kama toka mwanzo Mungu aliweza kuwaokoa watu hata toka matumboni mwa mama zao, kama Yohana, naye hakuwa na haja ya kafara ya Yesu, inaonekana hakukuwa na dhambi yo yote inayorithiwa inayohitaji ukombozi wa Yesu.

4. Habari za Melkizedeki, mfalme wa Salemi, kuhani wa Mungu aliye juu, zimeandikwa ya kwamba "hana baba, hana mama, hana wazazi, hana mwanzo, wa siku zake, wala mwisho wa uhai wake, ... adumu kuhani milele" (Waebrania 7:1-3). Huyu asiye na baba wala mama kama ingesemwa hakurithi dhambi ya asili, na ya kuwa aliwakomboa watu, labda watu wangeona kama maneno yamepatana, ingawa jambo lenyewe si sahihi. Lakini kusema aliyezaliwa na mwanamke mwenye wazazi waliorithi dhambi ndiye awe hana dhambi hiyo ya asili, ni kama kutaka kuwachezea watu wazima akili zao.

5. Katekisimu ya Katoliki inasema, "Watoto wadogo waliokufa na dhambi ya asili wasijeweza kutenda dhambi ingine, hatuoni kwamba watupwa Motoni pamoja na watu walaanifu. Watoto hao lakini, kwa sababu ya dhambi ya asili hutengwa kweli wasiingie Uwingu, wasimwone Mwenyezi Mungu' (uk. 38). Lakini maneno yao haya ni kinyume na maneno ya Yesu aliyosema,

"Waacheni vitoto, wala msiwakataze kuja kwangu; kwa maana walio mfano wa hao, ufalme wa mbinguni ni wao" (Matt. 19:14). Tena Yesu akasema, "Amin, nawaambieni, Msipoongoka na kuwa kama vitoto, hamtaingia kabisa katika ufalme wa mbinguni" (Matt. 18:2-3). Ni wazi Yesu mwenyewe hapa amekiri utakatifu wa watoto, ya kuwa watu wakiwa watakatifu kama watoto ndio wataingia mbinguni. Sasa watoto wenyewe wenye usafi unaoshuhudiwa na Yesu mwenyewe kwa nini wang'ang'anizwe dhambi ya asili ambayo hawana na kusemwa hawatamwona Mungu wala kuingizwa mbinguni?

6. Zaidi ya hayo Mungu hana haja kuwa mtu asiye na kosa auawe kwa kosa la watu wengine. Imeandikwa "Nafsi ya mtu ifanyayo dhambi ndiyo itakayokufa" (Ezekiel 18:4). Hivyo kusema Yesu asiye na kosa auawe kwa ajili ya madhambi ya watu ni jambo ambalo akili haikubali.

7. Mungu huweza kusamehe dhambi kwa kutubu tu bila kafara (2 Mambo ya Nyakati 7:12-14). Na mtu asiyetaja jina la Mungu kwa upuuzi anaweza kufanywa na Mungu awe hana kosa (Mwanzo 20:7). Yesu alisema, Mngalijua maana ya maneno haya, Nataka rehema wala si sadaka, hamngeliwalaumu wasio na hatia" (Matt. 12:7). Hivyo Mungu ni Mwenye rehema, huweza kuwasamehe watu bila mtu kujiua kama kafara badala yao.

8. Toka zamani njia za kuokoa watu si kwamba ye yote mwingine auawe kwa ajili ya dhambi zao; bali kwa matendo mema na ibada mtu huokoka. Hivyo utaona ya kuwa hata Yesu mwenyewe alisali na kufunga (Matt. 17:21; 4:2); akawaagiza wanafunzi wake wafunge (Matt. 6:16-18; Luka 5:35). Paulo naye akawaagiza watu kufunga na kuomba (1 Wakor. 7:5), nayo ni desturi inayoshikwa hata leo na baadhi ya Wakristo. Yesu alisema ya kuwa njia ya uongofu ni nyembamba (Matt. 7:13), na ingekuwa mtu anaokoka kwa sababu mtu fulani amejitoa kwa ajili yake, kama wasemavyo Wakristo, basi njia ya wokovu ingekuwa pana sana hata kuliko njia ya upotevu; wala pasingekuwa haja ya kusali na kufunga. Ingekuwa njia ya kawaida ya kuwaokoa watu imefungwa, na njia nyingine ya kafara ya Yesu ikaletwa, basi Yesu baada ya kuchukua dhambi za watu wengine, asingeweza kuokoka nafsi yake mpaka mtu mwingine aje ajitoe kafara kwa ajili yake. Kwa njia hii kafara isingekuwa na ukomo.

9. Katika Marko (9:43-48) na Ufunuo (14:11), imeandikwa ya kwamba anayekwenda Jahanamu hukaa humo milele. Kama ni kweli Yesu alichukua dhambi za watu wote, basi ni adhabu gani aliyopewa? Kama alitiwa Jahanamu kwa siku tatu tu kama wanavyotueleza Wakristo, hiyo haitoshi. Maana yeye amechukua dhambi za vizazi vyote vilivyopita, vilivyopo na vitakavyokuja kumwamini. Yeye alistahili aungue huko Jahanamu milele. Lakini kama Mungu alimtoa haraka haraka, basi ama Mungu hakufanya haki, wengine wakiwa na dhambi wanawaka milele, na Yesu aliyechukua dhambi zaidi kuliko kila mwenye dhambi aunguzwe siku tatu tu. Lakini kama Mungu ni mwadilifu, na Yesu ametoka Jahanamu, basi tena hakumaliza hata dhambi za watu kidogo katika wafuasi wake. Na hivi ndivyo tuonavyo. Wakristo wa kila upande wanazidi sana katika madhambi; umalaya, ulevi na kamari ni vitu vinavyoendeshwa katika nchi zao, na vita na magomvi, yanaendelea. Sasa ni dhambi gani alizowaondolea?

10. Yesu mwenyewe alikataa kuitwa mwema (Luka 18:19). Na imeandikwa ya kwamba aliyezaliwa na mwanamke hawezi kuwa mwema (Ayubu 25:4; 15:14). Kama mtu mwema hawezi kuondoa dhambi za wengine kwa kufa kwake, seuze asiye mwema!

11. Kama Yesu angekuja ili auawe, ili watu wasamehewe kwa kuadhibiwa yeye, asingekuwa na haja ya kuhubiri na kuweka wanafunzi. Asingekuwa na haja ya kungoja akamatwe na maadui zake, wamtie mahakamani na huko ahukumiwe kuuawa; angejitundika mtini mwenyewe ili kuwafia watu. Yesu angekuja kuwafia watu asingeogopa kuuawa wala asingeomba kwa Mungu kuwa ikiwezekana asinyweshwe kikombe cha mauti (Matt. 26:39; Marko 14:36; Luka 22:42). Maneno ya vifungu hivyo yanaonyesha Yesu hakutaka kufa. Sasa kuna kafara gani ya mtu kushurutishwa na kuadhibiwa hali mwenyewe hataki? Tunaona watu wa kawaida tu wanavumilia mateso, hata wanajiua kwa furaha, bila kuhangaika alivyohangaika Yesu. Huyu "mwana" wa Mungu alikuwa mwoga namna hii hata kuliko wanadamu wa kawaida! Kama ni kweli alipenda

kujitoa afie watu, ambavyo ni sawa na kusema, daktari ajivunje kichwa chake kwa nyundo ili wagonjwa wake wapone, kwa nini tena alipokuwa msalabani alilia, "Eloi, Eloi, lama sabakthani" yaani, Mungu wangu, Mungu wangu, mbona umeniacha? (Matt. 27:46). Wako watu wanaokufa mashahidi na wanakufa kwa kufurahi. Hata askari wanaopigania nchi yao wanakufa kwa furaha. Lakini huyu Bwana Yesu alitakaje kuwafia watu huku analia aachiliwe?

12. Isitoshe Yuda Eskariote aliyemsaliti Yesu alistahili heshima kubwa kwa Wakristo, maana yeye ndiye alimtambulisha Yesu hata akafika kukamatwa. Inaonekana kwa maelezo ya Injili, Yesu alijificha na kujibadili kwa namna ambayo maadui zake wasiweze kumtambua, ikabidi wamrubuni mwanafunzi wake mmoja waende naye akamtambulishe. Yuda Eskariote, alirubuniwa kwa vipande thelathini vya fedha, akakubali kuwapeleka Mayahudi akamtambulishe Yesu. Basi kwa nini huyu Yuda asiitwe mwokozi wa pili wa watu kwa kumkamatisha Yesu aliyekuwa anajificha? Kwa nini Wakristo wanamlaani na kusema "alianguka kifudifudi akapasuka, matumbo yake yote yakatoka" kwa sababu ya uovu wake wa kumsaliti Yesu?

Maelezo hayo yanatosha kuhakikisha ya kuwa hakuna mtu anayezaliwa na dhambi. Kila mtu anazaliwa safi kabisa, kwa kuwa ameumbwa kwa umbo lililo bora. Mtume s.a.w. alisema, "Hakuna mtoto anayezaliwa ila amezaliwa juu ya asili iliyo safi, lakini ni wazazi wake wanaomfanya kuwa Myahudi au Mkristo au Mmajusi" (Bukhari).

Tazameni sasa tofauti kubwa kati ya dini ya Kiislamu na Ukristo. Kwa hakika ni ihsani ya dini ya Kiislamu kusimamisha heshima ya mwanadamu kwa kutangaza ya kuwa amezaliwa safi pasipo dhambi yo yote. Lakini Ukristo unamwaibisha sana mwanadamu kwa kusema amezaliwa na dhambi ambazo hakupata kuzifanya. Kwa kweli mafundisho ya Kiislamu ndiyo yaliyo sawa na akili na sawa na asili ya mwanadamu, na ndiyo yanayostahili kufuatwa.

سُوْرَةُ الْعَلَقِ مَكِّيَّةٌ وَّ هِيَ مَعَ الْبَسْمَلَةِ عِشْرُوْنَ اٰيَةً وَّ رُكُوْعٌ

96. SURA AL'ALAQ

Imeteremshwa Makka

Ina Aya 20 pamoja na Bismillahi

بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ ①

1. Kwa jina la Allah, Mwingi wa rehema, Mwingi wa ukarimu.

اِقْرَاْ بِاسْمِ رَبِّكَ الَّذِىْ خَلَقَ ②

2. Soma kwa jina la Mola wako Aliyeumba.

خَلَقَ الْاِنْسَانَ مِنْ عَلَقٍ ③

3. Alimwumba mwanadamu kwa tone la damu iliyoganda.

اِقْرَاْ وَرَبُّكَ الْاَكْرَمُ ④

4. Soma! na Mola wako ni Mwenye heshima kuliko wote.

الَّذِىْ عَلَّمَ بِالْقَلَمِ ⑤

5. Ambaye Alifundisha kwa njia ya kalamu.

عَلَّمَ الْاِنْسَانَ مَا لَمْ يَعْلَمْ ⑥

6. Alimfunza mwanadamu asiyoyajua.

كَلَّآ اِنَّ الْاِنْسَانَ لَيَطْغٰٓى ⑦

7. Tahadhari! Kwa hakika mwanadamu ni mwenye kuasi.

اَنْ رَّاٰهُ اسْتَغْنٰى ⑧

8. Kwa kuwa anajiona yeye si mhitaji.

اِنَّ اِلٰى رَبِّكَ الرُّجْعٰى ⑨

9. Bila shaka marudio ni kwa Mola wako

اَرَءَيْتَ الَّذِىْ يَنْهٰى ⑩

10. Je! Umemwona akatazaye,

Sura hii ilishuka Makka na wanazuoni wote wanakubaliana.

Aya 2-6. Aya hizi tano ni chanzo cha Wahyi wa Mtume *s.a.w.*

Imam Ahmad amesimulia katika Musnad yake ya kuwa Mtume *s.a.w.* alikuwa akienda kaa faraghani katika pango la Hira, akimkumbuka Mungu. Siku moja Malaika Jibril akafika na akamwambia: *Iqra'* (Soma). Mtume *s.a.w.* anasema, nikajibu, "Mimi sijui kusoma." "Malaika Jibril akanishika na akanibana sana hata nguvu yangu ikaisha. Akaniachia. Akasema, Soma. Nikajibu, Mimi sijui kusoma. Akanishika akanibana sana, hata nguvu ikaniishia, na akaniacha, na akaniambia tena, Soma kwa jina la Mola wako aliyeumba." Imam Bukhari pia amesimulia tukio hili. Ibni Abbas anasimulia ya kwamba sura hii ndiyo ya kwanza kushuka katika Qur'an (Fat'hul Bayan). Inaonekana ya kwamba dini ya Kiislamu ni dini ya elimu, amani na ustaarabu. Kama makafiri wasingewashurutisha Waislamu wa kwanza kujikinga na upanga Uislamu ungefaulu bila ya kushughulika na mambo ya vita.

عَبْدًا اِذَا صَلّٰى ﴿١١﴾

11. Mtumishi (wa Mungu) asalipo?

اَرَءَيْتَ اِنْ كَانَ عَلَى الْهُدٰٓى ﴿١٢﴾

12. Je umetafakari (kuwa itakuwaje) kama yeye (mja wa Mungu) awe juu ya mwongozo?

اَوْ اَمَرَ بِالتَّقْوٰى ﴿١٣﴾

13. Au anaamuru ucha Mungu?

اَرَءَيْتَ اِنْ كَذَّبَ وَتَوَلّٰى ﴿١٤﴾

14. Je ulitafakari kuwa kama (yule mzuia sala) angekadhibisha (tena) na kukengeuka

اَلَمْ يَعْلَمْ بِاَنَّ اللّٰهَ يَرٰى ﴿١٥﴾

15. (Hivyo) hajui ya kuwa Allah Anaona?

كَلَّا لَئِنْ لَّمْ يَنْتَهِ ۙ لَنَسْفَعًۢا بِالنَّاصِيَةِ ﴿١٦﴾

16. Tahadhari! Kama haachi, Tutam-kokota kwa nywele za paji (lake),

نَاصِيَةٍ كَاذِبَةٍ خَاطِئَةٍ ﴿١٧﴾

17. Nywele za paji lenye uwongo, lenye dhambi.

فَلْيَدْعُ نَادِيَهٗ ﴿١٨﴾

18. Basi na awaite wenzake wa vikao vyao,

سَنَدْعُ الزَّبَانِيَةَ ﴿١٩﴾

19. Nasi Tutawaita Mazabania (ma-laika wa jehannam).

كَلَّا ۫ لَا تُطِعْهُ وَاسْجُدْ وَاقْتَرِبْ ﴿٢٠﴾ ۩

20. Tahadhari! Usimtii na usujudu na (jitahidi) uupate ukaribu (na Mungu).

Aya hizi zaonyesha jinsi Qur'an itakavyoendeleza elimu na kuwafundisha mambo yaliyofichikana zamani. Miaka michache tu baada ya kuteremshwa Aya hizi elimu za kuandika na kusoma zilizidi katika Bara Arabu, na pole pole Waarabu waliovumbikwa na giza la ujinga zamani wakawa waalimu wa mataifa yote, wakaumulika ulimwengu sawa na nyota. Waislamu waliwaamsha watu wa Ulaya, wakawafunza namna nyingi za elimu kama hesabu, utabibu, falaki, sanaa, ujenzi na kuogelea maji. Hawakugundua akili ya kutengeneza mashine ya kuvipiga chapa vitabu, lakini waliandika kwa kalamu vitabu maelfu na maelfu juu ya elimu kadha wa kadha, wakawa wavumbuzi wenye kushangaza dunia nzima.

Ummi kama Mtume Muhammad *s.a.w.* aweza kujidai kwamba atawafundisha kwa "kalamu" yale wasiyoyajua na yafanyike vile alivyosema, je, maneno haya hayakutoka katika kinywa cha Mungu Mjuzi na Mweza wa yote?

Aya 16. Huyu anayesemwa hapa ni Abu Jahal, mmoja katika makafiri wakubwa wa siku za Mtume waliokuwa maadui sana. Katika vita vya Badri aliuawa na alikokotwa kwa nywele za paji la uso wake na akatupwa shimoni; na bishara hii iliyotajwa hapa ikatimia.

سُوْرَةُ الْقَدْرِ مَكِّيَّةٌ وَّ هِيَ مَعَ الْبَسْمَلَةِ سِتُّ اٰيَاتٍ وَّ رُكُوْعٌ

97. SURA AL-QADR

Imeteremshwa Makka

Ina Aya 6 pamoja na Bismillahi

بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ ①

1. Kwa jina la Allah, Mwingi wa rehema, Mwingi wa ukarimu.

اِنَّاۤ اَنْزَلْنٰهُ فِيْ لَيْلَةِ الْقَدْرِ ۚ ②

2. Hakika Tumeiteremsha (Qur'an) katika usiku wa heshima.

وَمَاۤ اَدْرٰىكَ مَا لَيْلَةُ الْقَدْرِ ۙ ③

3. Na nini kitakujulisha usiku wa heshima ni nini?

لَيْلَةُ الْقَدْرِ ۙ خَيْرٌ مِّنْ اَلْفِ شَهْرٍ ؕ ④

4. Usiku wa heshima ni bora kuliko miezi elfu.

تَنَزَّلُ الْمَلٰٓئِكَةُ وَالرُّوْحُ فِيْهَا بِاِذْنِ رَبِّهِمْ ۚ مِنْ كُلِّ اَمْرٍ ۙ ⑤

5. Huteremka humo malaika kwa wingi na roho takatifu kwa amri ya Mola wao kuhusiana na kila jambo.

سَلٰمٌ ۛ هِيَ حَتّٰى مَطْلَعِ الْفَجْرِ ۧ ⑥

6. Amani - na (silsila hii) itakuwa hivyo mpaka mapambazuko ya alfajiri.

Abdullah bin Abbas na Abdullah bin Zubair na Bibi Aisha, wote wanasema ya kuwa sura hii ilishuka Makka.

Aya 2. *Usiku wa heshima.* Katika sura 2:186 imesemwa ya kuwa Qur'an ilishuka katika mwezi wa Ramadhani. na katika sura hii inasemwa ya kuwa iliposhuka ilishuka katika usiku unaoitwa *Lailat al-Qadir,* yaani usiku wenye heshima. Sio mradi wake kuwa Qur'an yote ilishuka katika mwezi mmoja au usiku ule mmoja, bali mwanzo wa kushuka ilikuwa ni katika usiku wa *Qadr* wa mwezi wa Ramadhani na ikaendelea kushuka kwa miaka 23.

Siku moja Mtume aliambiwa na Allah usiku huu ni tarehe gani ya mwezi wa Ramadhani. Alipokuwa akitoka ili kuwapa watu habari akakuta watu wanagombana na akaingilia kuwaamua. Katika kuwaamua, tarehe ile akaisahau, lakini akasema watu wanaweza kuitafuta *Lailat al-Qadr* katika tarehe 21 au 23 au 25 au 27 au 29 ya mwezi wa Ramadhani (Bukhari). *Lailat al-Qadir* huendelea mpaka alfajiri, ndiyo mwisho.

سُوْرَةُ الْبَيِّنَةِ مَدَنِيَّةٌ وَّ هِيَ مَعَ الْبَسْمَلَةِ تِسْعُ اٰيَاتٍ وَّ رُكُوْعٌ

98. SURA AL-BAYYINA

Imeteremshwa Madina

Ina Aya 9 pamoja na Bismillahi

بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ ①

1. Kwa jina la Allah, Mwingi wa rehema, Mwingi wa ukarimu.

لَمْ يَكُنِ الَّذِيْنَ كَفَرُوْا مِنْ اَهْلِ الْكِتٰبِ وَالْمُشْرِكِيْنَ مُنْفَكِّيْنَ حَتّٰى تَاْتِيَهُمُ الْبَيِّنَةُ ②

2. Wale waliokufuru miongoni mwa watu wa Kitabu na washirikina hawakuwa wenye kuacha asilan, juu ya kwamba dalili bayana zilikwisha wafikia.

رَسُوْلٌ مِّنَ اللّٰهِ يَتْلُوْا صُحُفًا مُّطَهَّرَةً ③

3. (Ni) Mtume aliyetoka kwa Allah aliyekuwa akiwasomea sahifa zilizotakasika.

فِيْهَا كُتُبٌ قَيِّمَةٌ ④

4. Ndani yake mna mafundisho ya kudumu.

وَمَا تَفَرَّقَ الَّذِيْنَ اُوْتُوا الْكِتٰبَ اِلَّا مِنْۢ بَعْدِ مَا جَآءَتْهُمُ الْبَيِّنَةُ ⑤

5. Wala hawakufarakiana wale waliopewa Kitabu ila baada ya kuwafikia (dalili) bayana.

وَمَآ اُمِرُوْٓا اِلَّا لِيَعْبُدُوا اللّٰهَ مُخْلِصِيْنَ لَهُ الدِّيْنَ ۙ حُنَفَآءَ وَ يُقِيْمُوا الصَّلٰوةَ

6. Wala hawakuamrishwa ila kumwabudu Allah kwa kumhalisishia dini kwa haki na kusimamisha Sala na kutoa Zaka:

Wanazuoni wengi wanakubali ya kuwa sura hii ilishuka Madina.

Aya 3. Katika Aya ya 2 ilisemwa ya kuwa watu wa Kitabu na washirikina hawakuwa wenye kuacha kufuru mpaka ingewafikia dalili iliyo wazi. Sasa katika Aya hii inaelezwa ya kuwa kila dalili haiwezi kuwafaa na kuwatoa katika kufuru kuwapeleka kwenye mwongozo. Kwa sababu hii Allah hakusema, *Hataa ta'tiyahum bayyinatun* bali amesema *Hattaa ta'tiyahumul bayyinatu,* yaani ametia tamko la *al* pia juu ya *bayyinah* kwa kuonyesha ya kuwa katika hali za kufuru za namna hii, watu hawawezi kuongoka kwa dalili na hoja, bali hutakiwa dalili wazi iliyo maalumu, yaani aje Nabii anayeweza kuwafaa na kuwapa msaada mkubwa kwa kuwatoa watu katika kufuru na uharibifu, na kuwapeleka kwenye mwongozo na wema; maana, bila Mtume wa Mungu kazi kubwa ya namna hii haiwezi kufanyika kwa hoja na vitabu tu.

Aya 4. *Kutubun qayyimah,* :Sheria madhubuti," yaani mambo yote mazuri yaliyotajwa zamani na mengine yasiyotajwa yote yamo katika Qur'an.

na hii ndiyo dini madhubuti.

وَيُؤْتُوا الزَّكٰوةَ وَذٰلِكَ دِيْنُ الْقَيِّمَةِ ۝٥

7. Bila shaka wale waliokufuru miongoni mwa watu wa Kitabu na washirikina watakuwa ndani ya moto wa Jahanamu, watakaa humo kwa muda mrefu; hao ndio viumbe wabaya kabisa kuliko viumbe vyote.

اِنَّ الَّذِيْنَ كَفَرُوْا مِنْ اَهْلِ الْكِتٰبِ وَالْمُشْرِكِيْنَ فِيْ نَارِ جَهَنَّمَ خٰلِدِيْنَ فِيْهَا ؕ اُولٰٓئِكَ هُمْ شَرُّ الْبَرِيَّةِ ۝٦

8. Hakika wale walioamini na walio tenda mema, hao ndio viumbe bora kuliko viumbe vyote.

اِنَّ الَّذِيْنَ اٰمَنُوْا وَعَمِلُوا الصّٰلِحٰتِ ۙ اُولٰٓئِكَ هُمْ خَيْرُ الْبَرِيَّةِ ۝٧

9. Malipo yao kwa Mola wao ni Bustani za daima zipitazo mito ndani yake; watakaa humo abadi; Allah Amewaridhia nao wamemridhia; (malipo) hayo ni kwa yule anayemwogopa Mola wake.

جَزَآؤُهُمْ عِنْدَ رَبِّهِمْ جَنّٰتُ عَدْنٍ تَجْرِيْ مِنْ تَحْتِهَا الْاَنْهٰرُ خٰلِدِيْنَ فِيْهَآ اَبَدًا ؕ رَضِيَ اللّٰهُ عَنْهُمْ وَرَضُوْا عَنْهُ ؕ ذٰلِكَ لِمَنْ خَشِيَ رَبَّهٗ ۝٨ ع ٢٣

Aya 9. Aya hii inaeleza sifa nzuri za masahaba wa Mtume *s.a.w.* ya kuwa Mungu amewaridhia na wao wamemridhia. Maneno haya yanavunja maneno ya watu wanaowasingizia masahaba wa Mtume *s.a.w.*

سُوْرَةُ الزِّلْزَالِ مَكِّيَّةٌ وَّ هِيَ مَعَ الْبَسْمَلَةِ تِسْعُ اٰيَاتٍ وَّ رُكُوْعٌ

99. SURA AZ-ZILZAAL

Imeteremshwa Makka

Ina Aya 9 pamoja na Bismillahi

بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ ①

1. Kwa jina la Allah, Mwingi wa rehema, Mwingi wa ukarimu.

اِذَا زُلْزِلَتِ الْاَرْضُ زِلْزَالَهَا ②

2. Itakapotetemeka ardhi kwa mtetemeko wake,

وَاَخْرَجَتِ الْاَرْضُ اَثْقَالَهَا ③

3. Na ardhi itakapotoa mizigo yake,

وَقَالَ الْاِنْسَانُ مَا لَهَا ④

4. Na mtu atasema: Oh! ina nini?

يَوْمَئِذٍ تُحَدِّثُ اَخْبَارَهَا ⑤

5. Siku hiyo itahadithia habari zake,

بِاَنَّ رَبَّكَ اَوْحٰى لَهَا ⑥

6. Itakuwa hivyo kwa sababu Mola wako Atakuwa Ameifunulia hivyo.

يَوْمَئِذٍ يَّصْدُرُ النَّاسُ اَشْتَاتًا ۙ لِّيُرَوْا اَعْمَالَهُمْ ⑦

7. Siku hiyo watu watatoka vikundi-vikundi ili waonyeshwe vitendo vyao.

فَمَنْ يَّعْمَلْ مِثْقَالَ ذَرَّةٍ خَيْرًا يَّرَهٗ ⑧

8. Basi atakayefanya wema sawa na chembe, atauona.

وَمَنْ يَّعْمَلْ مِثْقَالَ ذَرَّةٍ شَرًّا يَّرَهٗ ⑨ ع ۱۴

9. Na atakayefanya uovu sawa na chembe, atauona.

Mujahid, Ataa na Ibni Abbas wanasema ya kuwa sura hii ilishuka Makka. Lakini Katada na Mukatil wanasema ya kuwa sura hii ilishuka Madina. Basi kwa kuwa katika wenye kauli ya kwanza kuna sahaba mmoja, Ibni Abbas, anayesaidia kauli yao kuwa sura hii ilishuka Makka, hivyo tunaandika kuwa ilishuka Makka ingawa nakala za Qur'an za dunia nzima zinaonyesha ya kuwa sura hii ilishuka Madina.

Aya 2. Neno *zalzala* maana yake ni kutikisa, kutetemesha, kuhadharisha, kuogopesha na kuswaga. Neno *zalaazil* maana yake ni misiba na taabu (Akrab).

Aya 3. *Mizigo yake,* yaani madini za kila namna na hazina na elimu za mambo mengi vitatokea katika ardhi.

Aya 4. *Mtu,* yaani mtu ye yote atakayeiona ardhi imekwisha toa nje kila kilichofichikana ndani yake, atashangaa. Au mradi ni "mtu kamili" atakapoona hali ya ardhi, atashangaa.

سُوْرَةُ الْعَادِيَاتِ مَكِّيَّةٌ وَّ هِيَ مَعَ الْبَسْمَلَةِ اثْنَتَا عَشْرَةَ اٰيَةً وَّ رُكُوْعٌ

100. SURA AL-'AADIYAAT

Imeteremshwa Makka

Ina Aya 12 pamoja na Bismillahi

بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ ①

1. Kwa jina la Allah, Mwingi wa rehema, Mwingi wa ukarimu.

وَالْعٰدِيٰتِ ضَبْحًا ②

2. Naapa kwa (farasi) wakimbiaji wanaotweta,

فَالْمُوْرِيٰتِ قَدْحًا ③

3. Na kwa wale watoao moto kwa kupiga,

فَالْمُغِيْرٰتِ صُبْحًا ④

4. Tena kwa wale washambuliao wakati wa asubuhi,

فَاَثَرْنَ بِهٖ نَقْعًا ⑤

5. Basi hao wanatimua mavumbi.

فَوَسَطْنَ بِهٖ جَمْعًا ⑥

6. Kisha wanapenya hadi katikati ya majeshi ya adui:

اِنَّ الْاِنْسَانَ لِرَبِّهٖ لَكَنُوْدٌ ⑦

7. Bila shaka mtu ni mwenye kutoshukuru sana kwa Mola wake.

Ibni Mas'ud, Jabir, Al-Hasan, Ikrama na Ataa wanasema ya kuwa sura hii ilishuka Makka.

Aya 2. *Dhabhan* ni namna moja ya mbio za wanyama (Mufradat); tena ni sauti maalumu inayotoka katika vifua vya farasi wanapokimbia (Akrab).

Wakimbiaji wanaotweta, mradi wa maneno haya ni farasi. Abdullah bin Abbas na wanazuoni wengine kama Mujahid, Ikrama, Ataa, Qatada na Dhahhaak wote wanakubali ya kuwa mradi ni farasi. Na lugha ya Kiarabu pia inasaidia maana hii.

Iliposhuka sura hii watu walikuwa na ngamia, na hakukuwa sana desturi ya kuwatumia farasi. Lakini Allah kwa kuiteremsha Aya "Wakimbiaji wanaotweta" akabashiri ya kuwa hawa watu wa Makka wapandao ngamia siku moja watakuwa wapandao farasi. Na kweli, baadaye desturi ya kuwapanda farasi ilienea sana, na farasi wakazidi kabisa, na Waislamu wakawa wakimbiaji juu ya farasi katika matukio ya vita na amani. Kwa neno zima, Aya hii inajulisha ya kuwa Waislamu walikuwa na shauku na huba sana ya kuitumikia dini, hata wakawabana maadui waliokuwa na nguvu nyingi na silaha kubwa. Wao walikuwa wanakwenda mbio na wakiwakimbiza farasi kwa kutoa sadaka maisha yao.

Aya 7. *Kanuud.* Neno hili linatumiwa kwa mwanamume na mwanamke. Lina maana hizi: asiye na shukrani; akataaye neema za Allah; kafiri na mtu anayemlaumu Mola wake (Akrab); pia maana yake ni: mtu mchoyo, ardhi isiyozaa cho chote, mtu anayekula peke

8. Naye hasa ni shahidi wa hayo. وَاِنَّهٗ عَلٰى ذٰلِكَ لَشَهِيْدٌ ۚ﴿٨﴾

9. Naye kwa hakika ana mapenzi sana na mali. وَاِنَّهٗ لِحُبِّ الْخَيْرِ لَشَدِيْدٌ ؕ﴿٩﴾

10. Je, hajui watakapofufuliwa waliomo makaburini, اَفَلَا يَعْلَمُ اِذَا بُعْثِرَ مَا فِى الْقُبُوْرِ ۙ﴿١٠﴾

11. Na yatakapodhihirishwa yaliyomo vifuani? وَحُصِّلَ مَا فِى الصُّدُوْرِ ۙ﴿١١﴾

12. Hakika Mola wao Atawajua sana Siku hiyo. اِنَّ رَبَّهُمْ بِهِمْ يَوْمَئِذٍ لَّخَبِيْرٌ ۛ﴿١٢﴾ ع ١٢/١٥

---

yake na bahili na mtu anayempiga mtumwa wake (Akrab). Hata maana hii imeelezwa katika Hadithi. Abi Umama anasema ya kuwa Mtume *s.a.w.* alisema ya kuwa *kanuud* ni mtu anayekula peke yake na anampiga mtumwa wake na hatoi kitu kuwapa wengine (Ibni Kathir). Katika kitabu cha kamusi kiitwacho *Taarifaat* mmeandikwa ya kuwa *kanuud* ni "ambaye anaihesabu misiba na kusahau mema".

Mtu. Siyo mradi hapa kila mtu, bali ni wale tu watakaoshambuliwa na Waislamu ambao wametajwa katika Aya ya 6. Hao ndio watakaokuwa wenye tabia za namna hii zilizoelezwa ndani ya neno la *kanuud* - makafiri, wachoyo, wadhalilifu, wenye tabia mbaya na wasio na shukrani, waoga na zaidi ya hayo hawakuwa wenye kutoa mali zao kwa kuwasaidia wenye haja, bali walikuwa wanaowapiga wanawake na watumwa.

Aya 8. Na juu ya hayo wanajivuna na wanasema wamefanya mambo kadha wa kadha.

سُوْرَةُ الْقَارِعَةِ مَكِّيَّةٌ وَّ هِيَ مَعَ الْبَسْمَلَةِ اثْنَتَا عَشْرَةَ اٰيَةً وَّ رُكُوْعٌ

101 SURA AL-QAARI'A

Imeteremshwa Makka

Ina Aya 12 pamoja na Bismillahi

بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ ①

1. Kwa jina la Allah, Mwingi wa rehema, Mwingi wa ukarimu.

اَلْقَارِعَةُ ②

2. (Msiba) ugongao!

مَا الْقَارِعَةُ ③

3. (Msiba) ugongao ni nini?

وَمَآ اَدْرٰىكَ مَا الْقَارِعَةُ ④

4. Na nini kitakujulisha (msiba) ugongao ni nini?

يَوْمَ يَكُوْنُ النَّاسُ كَالْفَرَاشِ الْمَبْثُوْثِ ⑤

5. Siku ambayo watu watakuwa kama nondo waliotawanywa,

وَتَكُوْنُ الْجِبَالُ كَالْعِهْنِ الْمَنْفُوْشِ ⑥

6. Na milima itakuwa kama sufu zilizochambuliwa.

فَاَمَّا مَنْ ثَقُلَتْ مَوَازِيْنُهٗ ⑦

7. Basi ama yule ambaye mizani yake itakuwa nzito,

فَهُوَ فِيْ عِيْشَةٍ رَّاضِيَةٍ ⑧

8. Basi huyo atakuwa katika maisha yanayopendeza.

وَاَمَّا مَنْ خَفَّتْ مَوَازِيْنُهٗ ⑨

9. Na ama yule ambaye mizani yake itakuwa hafifu,

فَاُمُّهٗ هَاوِيَةٌ ⑩

10. Basi mama yake atakuwa 'Haawiyah'.

وَمَآ اَدْرٰىكَ مَا هِيَهْ ⑪

11. Na nini kitakujulisha Haawiya ni nini?

نَارٌ حَامِيَةٌ ⑫ ع ۱۱

12. Ni Moto uwakao!

Wanazuoni wanakubaliana kuwa sura hii ilishuka Makka.

Aya 7. Mizani ya vitendo vyake vizuri ikiwa nzito zaidi kuliko uzito wa vitendo vyake vibaya ndipo mtu atasalimika.

Aya 10. *Fa ummuhuu haawiyah,* "Mama yake ni Haawiya." Pia inaweza kutafsiriwa "makao yake ni Haawiya." Haawiya ni daraja ya chini kabisa katika shimo la Jahanamu. Hapa Jahanamu imeitwa "mama" na muradi wake ni kuwa kama vile mtoto mchanga anavyotaraji kuwa pamoja na mama yake ili alelewe apate kufikia maisha ya ujana na kukaa huru peke yake, kadhalika mtu mwovu anataraji kwanza kulelewa ndani ya Jahanamu na kutibiwa maradhi yake; baadaye atakapopona atatolewa nje ya moto na kupelekwa Peponi.

سُوْرَةُ التَّكَاثُرِ مَكِّيَّةٌ وَّ هِيَ مَعَ الْبَسْمَلَةِ تِسْعُ اٰيَاتٍ وَّ رُكُوْعٌ

102. SURA AT-TAKAATHUR

Imeteremshwa Makka

Ina Aya 9 pamoja na Bismillahi

بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ ①

1. Kwa jina la Allah, Mwingi wa rehema, Mwingi wa ukarimu.

اَلْهٰىكُمُ التَّكَاثُرُ ②

2. Yamekughafilisheni mashindano yenu ya kujilundikia mali,

حَتّٰى زُرْتُمُ الْمَقَابِرَ ③

3. Kiasi ya kwamba mmeyazuru hata makaburi.

كَلَّا سَوْفَ تَعْلَمُوْنَ ④

4. Tahadharini! karibuni mtajua.

ثُمَّ كَلَّا سَوْفَ تَعْلَمُوْنَ ⑤

5. Tena tahadharini! hivi karibuni mtajua.

كَلَّا لَوْ تَعْلَمُوْنَ عِلْمَ الْيَقِيْنِ ⑥

6. Sivyo! Lau mngaliijua elimu ya yakini:

لَتَرَوُنَّ الْجَحِيْمَ ⑦

7. Hakika mtaiona jahanamu:

ثُمَّ لَتَرَوُنَّهَا عَيْنَ الْيَقِيْنِ ⑧

8. Kisha hakika mtaiona kwa jicho la yakini:

ثُمَّ لَتُسْـَٔلُنَّ يَوْمَئِذٍ عَنِ النَّعِيْمِ ⑨ ع ۹ ۲۷

9. Kisha kwa hakika mtaulizwa Siku hiyo juu ya neema (mlizopewa).

Wanazuoni wengi zaidi wanakubaliana ya kuwa sura hii ilishuka Makka. Imam Bukhari anaeleza ya kuwa ilishuka Madina. Lakini sahaba mmoja, Ibni Abbas, anasema ya kuwa ilishuka Makka.

Aya 2. Neno *Takaathur* anasema Ibn Abbas maana yake ni tamaa nyingi ya mali na watoto (Bukhari). Abu Huraira anasimulia ya kuwa Mtume s.a.w. aliposoma sura hii alisema, "Mwanadamu anasema, hii ni mali yangu, hii ni mali yangu. Kumbe aliyokula na kuvaa ameichakaza, aliyotoa katika njia ya Allah, ndiyo kaiweka akiba na iliyobaki si yake ni mali ya watu."

Aya 6. *Yakini.* Yakini ina madaraja matatu. Mawili yametajwa hapa na moja limetajwa katika sura 56:96. (1) *'Ilmul yaqiin* ni yakini ya kujua kwa elimu: kama vile kuona moshi kwa mbali mtu akafahamu kuwa kuna moto. Pengine moshi ule unaweza kuwa ni vumbi tu au ukungu, basi daraja hii ya yakini ni ndogo. (2) *'Ainul yaqiin* ni yakini ya kuona kwa jicho, kama vile kuuona moto wenyewe hasa ukiwaka; na daraja ya (3) inaitwa *Haqqul yaqiin* yaani yakini iliyohakikishwa kwa kutia kidole motoni na kuhisi nguvu yake ya kuunguza au kuchoma.

سُوْرَةُ الْعَصْرِ مَكِّيَّةٌ وَّ هِيَ مَعَ الْبَسْمَلَةِ اَرْبَعُ اٰيَاتٍ وَّ رُكُوْعٌ

103. SURA AL-'ASR

Imeteremshwa Makka

Ina Aya 4 pamoja na Bismillahi

بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ ①

1. Kwa jina la Allah, Mwingi wa rehema, Mwingi wa ukarimu.

وَالْعَصْرِ ۙ ②

2. Naapa kwa Alasiri (zama),

اِنَّ الْاِنْسَانَ لَفِيْ خُسْرٍ ۙ ③

3. Kwa hakika mtu yumo hasarani,

اِلَّا الَّذِيْنَ اٰمَنُوْا وَعَمِلُوا الصّٰلِحٰتِ وَتَوَاصَوْا بِالْحَقِّ ۙ وَتَوَاصَوْا بِالصَّبْرِ ④

4. Isipokuwa wale walioamini na wakafanya vitendo vizuri, na wakausiana (kushika) haki na wakausiana (kushika) subira.

ع ١ ١٨

Wafasiri wengi wanasema sura hii ilishuka Makka.

Imam Shafii anasema, Sura hii ina maana nyingi na pana. Na kama mtu aifikiri, haja zake zote za dini zinaweza kutimizwa.

Imesimuliwa katika Hadithi ya kuwa masahaba wawili kila mara walipokuwa wanakutana wakati wa kuagana walikuwa wakisomeana sura hii.

Aya 2. *Al-'Asr.* Neno hili maana yake ni wakati, wakati wa alasiri, na pia maana yake ni kukamua.

Katika Aya hii Allah analeta ushahidi wa wakati kuonyesha ya kwamba kadiri wakati unavyopita umri wa kila mtu unapungua na kuingia katika hasara maana kila kitu kinasogelea mwisho wake na kitakufa. Lakini watu wanaweza kujiepusha na hasara hiyo kwa kuamini na kutenda mema na kuusiana kushika haki na subira, maana mambo haya yatafanya roho zao ziendelee katika maisha ya raha huko Akhera.

Katika sura hii habari za watu wa namna mbili zimeelezwa. Ya kwanza ni wale ambao wamo hasarani, na pili ni wale ambao wameamini na kufanya vitendo vizuri. Ni dhahiri ya kuwa wasioamini wala hawafanyi vitendo vizuri wao ndio watakaokuwa katika hasara. Lakini wanaoamini kwa moyo wote, tena wanaionyesha imani yao kwa viungo vyao, kwa kutenda sawa na walivyoamini, bila shaka wao watalindwa na hasara. Tena ikumbukwe ya kuwa Allah aliposema "walioamini" kwa hakika ameashiria kwenye ukamilifu wa elimu; maana imani haiwezi kupatikana bila elimu, Basi mtu anapopata ukamilifu katika elimu, anakuwa mwenye imani hasa. Na Allah aliposema "kufanya vitendo vizuri" ameelekeza kwenye ukamilifu wa amali, yaani matendo. Hivyo Allah amesema ya kuwa watu wanaokamilika katika elimu, na wanaokamilika katika vitendo, wao wanasalimika katika hasara na wanaokoka.

سُوْرَةُ الْهُمَزَةِ مَكِّيَّةٌ وَّ هِيَ مَعَ الْبَسْمَلَةِ عَشْرُ اٰيَاتٍ وَّ رُكُوْعٌ

104. SURA AL-HUMAZA

Imeteremshwa Makka

Ina Aya 10 pamoja na Bismillahi

بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ ①

1. Kwa jina la Allah, Mwingi wa rehema, Mwingi wa ukarimu.

وَيْلٌ لِّكُلِّ هُمَزَةٍ لُّمَزَةٍ ②

2. Maangamizo kwa kila msingiziaji,

الَّذِيْ جَمَعَ مَالًا وَّعَدَّدَهٗ ③

3. Aliyeikusanya mali na kuihesabu,

يَحْسَبُ اَنَّ مَالَهٗۤ اَخْلَدَهٗ ④

4. Alikuwa anadhani ya kuwa mali yake itamdumisha.

كَلَّا لَيُنْۢبَذَنَّ فِي الْحُطَمَةِ ⑤

5. Hasha! Bila shaka atavurumishwa katika Hutama.

وَمَاۤ اَدْرٰىكَ مَا الْحُطَمَةُ ⑥

6. Na nini kitakujulisha Hutama ni nini?

نَارُ اللّٰهِ الْمُوْقَدَةُ ⑦

7. Ni Moto wa Allah uliowashwa,

الَّتِيْ تَطَّلِعُ عَلَى الْاَفْـِٕدَةِ ⑧

8. Ambao utairukia mioyo,

اِنَّهَا عَلَيْهِمْ مُّؤْصَدَةٌ ⑨

9. Hakika huo utafunikwa dhidi yao,

فِيْ عَمَدٍ مُّمَدَّدَةٍ ⑩

10. Katika nguzo ndefundefu.

Wafasiri wengi wanakubaliana ya kuwa sura hii ilishuka Makka.

Hali ya watu wa siku za Mtume *s.a.w.* waliokuwa wakiwaudhi Waislamu na wakijivuna kwa mali zao, imeelezwa katika sura hii.

Aya 2. *Humazah,* "Msingiziaji." Neno hili limetoka katika neno *hamazah* lenye maana ya kusingizia; kukoneka; kupiga kwa kidole; kusukuma; kupiga; kuuma; kusengenya; kuvunja; kutia wasiwasi.

Lumazah (Msingiziaji) ni neno lililotoka katika *lamazah,* yaani kusingizia, kuaibisha; na kukoneka.

Masahaba na watu wa baadaye wamehitilafiana katika maana ya Aya hii, na hakuna sababu yake nyingine isipokuwa ya kwamba maneno haya mawili *humazah* na *lumazah* yanakaribiana sana katika maana. Inasemekana ya kuwa Mughira, A'as bin Wail na Sharik walikuwa wakishughulika kila mara kumwudhi Mtume *s.a.w.* na masahaba kwa kuwasingizia na kuwaaibisha; basi Allah katika sura hii akawaonya ya kuwa waache mwendo wao huo waila wataangamizwa.

Lakini hakuna haki ya kusema ya kuwa watu hawa watatu tu ndio walioonywa, maana wangekuwa ni hao watatu tu, basi wangetajwa majina yao. Lakini badala ya kutajwa majina yao Allah amesema, *Maangamizo kwa kila msingiziaji, msengenyaji.* Hili laonyesha ya kuwa watu wote wenye ada na mwendo wa namna hiyo wameonywa - wawe watu wa zamani, wa leo, hata na wa baadaye - wote watapata adhabu kutoka kwa Allah kwa dhambi zao za kuwasingizia, kuwaaibisha, kuwasengenya na kuwateta watu. Hivyo, Allah amewaonya watu wote wa siku zote ili wasishike njia ya namna hii inayoleta machafuko makubwa kati ya jamii za watu na makabila, na watu wanatenguka nguvu zao na kuangamia kabisa.

Aya 5. *Hutama* ni msiba unaosagasaga, na ni daraja ya pili ya Jahanamu, na pia ni moto uwakao.

سُوْرَةُ الْفِيْلِ مَكِّيَّةٌ وَّ هِيَ مَعَ الْبَسْمَلَةِ سِتُّ اٰيَاتٍ وَّ رُكُوْعٌ

105. SURA AL-FIIL

Imeteremshwa Makka

Ina Aya 6 pamoja na Bismillahi

بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ ①

1. Kwa jina la Allah, Mwingi wa rehema, Mwingi wa ukarimu.

اَلَمْ تَرَ كَيْفَ فَعَلَ رَبُّكَ بِاَصْحٰبِ الْفِيْلِ ②

2. Je! hukuona jinsi Mola wako Alivyowatenda watu wenye tembo?

اَلَمْ يَجْعَلْ كَيْدَهُمْ فِيْ تَضْلِيْلٍ ③

3. Je! Hakuiharibu hila yao?

وَّ اَرْسَلَ عَلَيْهِمْ طَيْرًا اَبَابِيْلَ ④

4. Na Akawapelekea juu yao ndege makundi-makundi,

تَرْمِيْهِمْ بِحِجَارَةٍ مِّنْ سِجِّيْلٍ ⑤

5. Wakawapiga mawe ya udongo uliookwa,

فَجَعَلَهُمْ كَعَصْفٍ مَّاْكُوْلٍ ⑥

6. Na Akawafanya kama majani makavu yaliyosagwa.

Aya 2-6. Habari zinazoelezwa hapa zilipita zamani katika Bara Arabu, kabla ya kuzaliwa Mtume *s.a.w.* Gavana mmoja wa mfalme wa Abisinia (Habeshi) aliyekuwa anatawala Yemen, alijenga kanisa moja zuri mahali panapoitwa Sanaa akitaka kuwazuia Waarabu kwenda fanya ibada zao kwenye Kaaba na waende huko kwenye kanisa lake, na ili biashara ya nchi yake izidi. Basi alikusanya jeshi ili kwenda kuivunja Kaaba Katika jeshi lile walikuwamo tembo mmoja au zaidi, na kwa sababu hii katika Bara Arabu wakaitwa *As-haabul-Fiil,* yaani wenye tembo. Jambo hili lilitokea katika mwaka 570, mwaka aliozaliwa Mtume *s.a.w.* Waarabu walipojua wanaendewa kushambuliwa na jeshi kubwa wakaona afadhali wakimbie wautoke mji. Bwana Abdul Muttalib, mkubwa wao, akaenda katika Kaaba, akashika pazia na akaomba, "Ee Mungu, ilinde Nyumba Yako na usiache msalaba kushinda Kaaba." Basi jeshi lile la Abraha lilifikwa na ugonjwa wa ndui na likaangamia (Soma, Life of Muhammad by Sir William Muir, introduction, p. c).

سُوْرَةُ قُرَيْشٍ مَكِّيَّةٌ وَّ هِيَ مَعَ الْبَسْمَلَةِ خَمْسُ اٰيَاتٍ وَّ رُكُوْعٌ

106. SURA QURAISH

Imeteremshwa Makka

Ina Aya 5 pamoja na Bismillahi

بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ ①

1. Kwa jina la Allah, Mwingi wa rehema, Mwingi wa ukarimu.

لِاِيْلٰفِ قُرَيْشٍ ②

2. Ili kuwaunganisha pamoja Waquraish

اٖلٰفِهِمْ رِحْلَةَ الشِّتَآءِ وَالصَّيْفِ ③

3. Na ili kukuza mwungano wao Tumebuni misafara ya kibiashara ya nyakati za kipupwe na kiangazi

فَلْيَعْبُدُوْا رَبَّ هٰذَا الْبَيْتِ ④

4. Basi wanatakiwa wamwabudu Bwana wa Jumba hili (Kaaba),

الَّذِيْٓ اَطْعَمَهُمْ مِّنْ جُوْعٍ ۙ وَّاٰمَنَهُمْ مِّنْ خَوْفٍ ⑤ ع ۳۱

5. Ambaye Anawalisha wakati wa njaa na Anawapa amani wakati wa hofu.

Sura hii ina majina mawili. Inaitwa Qureish na pia inaitwa *Li ii laafi.* Ibni Abbas anasimulia ya kuwa ilishuka Makka.

Aya 2. *Qureish* ni jina la kabila lililotoka kwa Nadhir bin Kinana (Razi). Wengine wanasema neno *Qureish* limetoka katika neno *Qarsh* ambalo ni jina la samaki mkubwa wa bahari anayekula samaki lakini yeye haliwi. Hivyo kwa ukubwa wa kabila lao na kwa kuheshimiwa na watu wote nao wakaitwa Kureish.

Makureish walikuwa watu wa Makka na walinzi wa Kaaba, na kwa sababu ya kuilinda Kaaba waliheshimiwa sana.

Aya 3. Wakati wa kipupwe (wakati wa baridi) walikuwa wakisafiri kwenda Afrika, bara Hindi na Yemen. Na wakati wa kiangazi walikuwa wakienda sham na Ajemi. Nyumba ya Kaaba iliposalimika bila kuharibiwa na Abraha, watu walizidi kuwaheshimu Wakureish kwa kuwa Mungu Anawaheshimu. Hivyo walikuwa wanafanya biashara zao kila mahali kwa kuheshimiwa.

Wamwabudu Bwana wa Jumba hili. Hawakuambiwa waiabudu nyumba bali wamwabudu Allah ambaye ni Bwana wa Kaaba. Na kwa sababu ni Nyumba iliyo ishara ya Allah ndiyo maana tunaiheshimu. Siku moja Seyidna Umar, Khalifa wa pili, alikuwa akiizunguka Kaaba na akalifikia Jiwe Jeusi. Akaligusa kwa fimbo yake akasema, "Mimi nina yakini kuwa wewe ni jiwe tu kama mawe mengine. Huna dhara wala huna manufaa. Lakini ninakubusu kwa sababu ni amri ya Allah."

Basi kwa neno zima, wakureish wanaambiwa katika Aya hizi ya kuwa wamependelewa na kupewa heshima kwa sababu ya kuilinda Nyumba ya Allah ambayo ni ya mawe na udongo tu basi itakuwa hali gani kama watamsaidia Mtume wa Mungu, bila shaka watapata heshima kubwa zaidi.

سُوْرَةُ الْمَاعُوْنِ مَكِّيَّةٌ وَّ هِيَ مَعَ الْبَسْمَلَةِ ثَمَانِيَ اٰيَاتٍ وَّ رُكُوْعٌ

107. SURA AL-MAA'UUN

Imeteremshwa Makka

Ina Aya 8 pamoja na Bismillahi

بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ ①

1. Kwa jina la Allah, Mwingi wa rehema, Mwingi wa ukarimu.

اَرَءَيْتَ الَّذِىْ يُكَذِّبُ بِالدِّيْنِ ②

2. Je, umemwona yule anayekadhibisha dini.

فَذٰلِكَ الَّذِىْ يَدُعُّ الْيَتِيْمَ ③

3. Basi huyo ndiye anayemsukuma yatima.

وَلَا يَحُضُّ عَلٰى طَعَامِ الْمِسْكِيْنِ ④

4. Wala hahimizi kuwalisha maskini.

فَوَيْلٌ لِّلْمُصَلِّيْنَ ⑤

5. Basi ole kwa wanaosali,

الَّذِيْنَ هُمْ عَنْ صَلَاتِهِمْ سَاهُوْنَ ⑥

6. Ambao wanapuuza Sala zao,

الَّذِيْنَ هُمْ يُرَآءُوْنَ ⑦

7. Ambao hufanya ili waonwe,

وَيَمْنَعُوْنَ الْمَاعُوْنَ ⑧

8. Na huwanyima watu hata faida ndogondogo.

Sura hii mbele ya wanazuoni wengi, ni ya Makka, na masahaba wengi pia wanakubali

Aya 2. *Anayekadhibisha dini.* Neno *Diin* kwa Kiarabu maana yake ni dini, malipo, utii, hukumu, ushindi, utawala, ufalme, hila, tabia, utakaso, hali na ada.

Aya 8. *Maa'uun* ni wema. Tena ni vitu vifaavyo kama moto, maji, chumvi, kibiriti, sahani n.k.w. (Razi). Pia neno hili maana yake ni Zaka, kwa kuwa ni sehemu ndogo tu ya mali inayotolewa. Ibn Abbas, Ikrama, na Katada walilifahamu hivyo neno hili (Razi na Kashshaf).

Abu Ubeida, sahaba wa Mtume *s.a.w.,* amesema ya kuwa *yamna'uunal-ma'uun,* muradi wake ni kuwa utii utatoka katika mioyo ya Waislamu na kila mmoja atajiona yeye ni yeye tu.

سُوْرَةُ الْكَوْثَرِ مَكِّيَّةٌ وَّ هِيَ مَعَ الْبَسْمَلَةِ اَرْبَعُ اٰيَاتٍ وَّ رُكُوْعٌ

108. SURA AL-KAUTHAR

Imeteremshwa Makka

Ina Aya 4 pamoja na Bismillahi

بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ ①

1. Kwa jina la Allah, Mwingi wa rehema, Mwingi wa ukarimu.

اِنَّآ اَعْطَيْنٰكَ الْكَوْثَرَ ②

2. Hakika Tumekupa heri nyingi.

فَصَلِّ لِرَبِّكَ وَانْحَرْ ③

3. Basi usali kwa Mola wako na utoe dhabihu.

اِنَّ شَانِئَكَ هُوَ الْاَبْتَرُ ④ ع ۱۳

4. Hakika adui yako atakuwa mkiwa.

Wanazuoni wengi wanaeleza ya kuwa sura hii ni ya Makka. Lakini Katada na Hassan Basri wanafahamu ya kuwa sura hii ni ya Madina.

Aya 2. *Kauthar,* "heri nyingi." Neno hili lina maana hizi: (1) uwingi wa kila kitu; (2) mkuu wa watu mwenye heri nyingi; (3) mtu mkarimu sana aenezaye wema mwingi; (4) *Kauthar* ni mto ulioko Peponi (Akrab). Inasemekana ya kuwa heri nyingi alizopewa Mtume *s.a.w*. ni Unabii na Qur'an. Sura hii inaonyesha ya kuwa kama mtu apate heri anatakiwa kumshukuru Allah kwa kusali na kutoa sadaka, ndipo atafanikiwa na maadui zake hawatamwangamiza.

سُوْرَةُ الْكَافِرُوْنِ مَكِّيَّةٌ وَّ هِيَ مَعَ الْبَسْمَلَةِ سَبْعُ اٰيَاتٍ وَّ رُكُوْعٌ

109. SURA AL-KAAFIRUUN

Imeteremshwa Makka

Ina Aya 7 pamoja na Bismillahi

بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ ①

1. Kwa jina la Allah, Mwingi wa rehema, Mwingi wa ukarimu.

قُلْ يٰٓاَيُّهَا الْكٰفِرُوْنَ ۙ②

2. Sema: Enyi makafiri!

لَآ اَعْبُدُ مَا تَعْبُدُوْنَ ۙ③

3. Siabudu mnachoabudu.

وَلَآ اَنْتُمْ عٰبِدُوْنَ مَآ اَعْبُدُ ۚ④

4. Wala ninyi hamumwabudu ninaye-mwabudu.

وَلَآ اَنَا عَابِدٌ مَّا عَبَدْتُّمْ ۙ⑤

5. Wala sitaabudu mnachoabudu.

وَلَآ اَنْتُمْ عٰبِدُوْنَ مَآ اَعْبُدُ ؕ⑥

6. Wala ninyi hamtamwabudu ninaye-mwabudu.

لَكُمْ دِيْنُكُمْ وَلِيَ دِيْنِ ۧ⑦

7. Ninyi mtapata malipo yenu nami nitapata malipo yangu.

Aya 7. *Malipo yenu.* Kama tulivyoeleza neno *Diin* pia maana yake ni malipo. Hivyo muradi wa Aya hii ni kuwa makafiri kwa kufuata dini yao watapata malipo wanayoyapata makafiri siku zote, na Mtume *s.a.w.* kwa kushika dini ya haki atapata malipo ambayo hupewa Manabii. Vivi hivi ndivyo mambo yalivyotokea. Makafiri waliadhibiwa na dini yao ikavunjika na Uislamu uliendelea.

سُوْرَةُ النَّصْرِ مَدَنِيَّةٌ وَّ هِيَ مَعَ الْبَسْمَلَةِ اَرْبَعُ اٰيَاتٍ وَّ رُكُوْعٌ

110. SURA AN-NASR

Imeteremshwa Madina

Ina Aya 4 pamoja na Bismillahi

بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ ①

1. Kwa jina la Allah, Mwingi wa rehema, Mwingi wa ukarimu.

اِذَا جَآءَ نَصْرُ اللّٰهِ وَالْفَتْحُ ②

2. Utakapofika msaada wa Allah na ushindi,

وَرَاَيْتَ النَّاسَ يَدْخُلُوْنَ فِيْ دِيْنِ اللّٰهِ اَفْوَاجًا ③

3. Na utawaona watu wakiingia dini ya Allah makundi-makundi,

فَسَبِّحْ بِحَمْدِ رَبِّكَ وَاسْتَغْفِرْهُ ؕ اِنَّهٗ كَانَ تَوَّابًا ④ ع

4. Basi Mtukuze Mola wako kwa sifa njema, na umwombe ghofira; hakika Yeye ndiye Apokeaye sana toba.

Sura hii inaitwa ya Madina kwa kuwa ilishuka baada ya Mtume kuhama ingawa iliposhuka ilikuwa ni katika Makka wakati Mtume alipokwenda kufanya Haji ya mwisho.

Aya 2. *Ushindi* mkubwa uliotajwa hapa ni ushindi wa Makka ilipoingia katika mamlaka ya Waislamu, mwaka wa 8 wa Hijra, na mwaka uliofuata ikawa makundi-makundi ya makabila ya Waarabu yanakuja ingia Uislamu. Hivi ndivyo Allah alivyotimiza bishara Zake za ajabu; na Mtume *s.a.w.* anaambiwa aombe ghofira kwa ajili ya makundi hayo yatakayoingia Uislamu maana kazi ya kusimamisha sheria ilikuwa kubwa. Seyidna Abu Bakar iliposhuka sura hii alilia. Watu wakamwuliza mbona unalia? Akajibu, Kazi ya Mtume *s.a.w.* sasa imekwisha na atatutoka.

سُوْرَةُ اللَّهَبِ مَكِّيَّةٌ وَّ هِيَ مَعَ الْبَسْمَلَةِ سِتُّ اٰيَاتٍ وَّ رُكُوْعٌ

111. SURA AL-LAHAB

Imeteremshwa Makka

Ina Aya 6 pamoja na Bismillahi

بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ ①

1. Kwa jina la Allah, Mwingi wa rehema, Mwingi wa ukarimu.

تَبَّتْ يَدَآ اَبِيْ لَهَبٍ وَّتَبَّ ②

2. Iangamie mikono miwili ya Abuu Lahab, naye pia aangamie.

مَآ اَغْنٰى عَنْهُ مَالُهٗ وَمَا كَسَبَ ③

3. Haitamfaa mali yake wala alivyovichuma.

سَيَصْلٰى نَارًا ذَاتَ لَهَبٍ ④

4. Hivi karibuni yeye ataungua katika Moto wenye mwako;

وَّامْرَاَتُهٗ ؕ حَمَّالَةَ الْحَطَبِ ⑤

5. Na mwanamke wake, aliye ni mchukuzi wa kuni,

فِيْ جِيْدِهَا حَبْلٌ مِّنْ مَّسَدٍ ⑥ ع

6. Shingoni mwake imo kamba iliyosokotwa.

Sura hii ni katika zile zilizoshuka mwanzoni Mtume alipokuwa Makka.

Aya 2. *Mikono miwili,* muradi wake ni dini yake na dunia yake (Razi) vyote vimeangamia. Huyu Abu Lahab jina lake hasa ni Abdul Uzza, naye alikuwa baba mdogo wa Mtume *s.a.w.* Neno *Abuu Lahab* - baba wa miali ya moto - ni jina ambalo hutumika kwa ajili ya mtu ambaye hali yake ya asili ni ya moto na ya uasi, na pia hutumika kwa ajili ya mtu ambaye anawachochea wengine. Hivyo bwana huyu amepangwa jina hili na Qur'an kwa sababu ya uadui wake kwa Mtume *s.a.w.* Siku ya kwanza Mtume s.a.w. alipowaita Wakureishi ili kuwaeleza habari za ujumbe wake, huyu Abu Lahab, alimkaripia akasema, "Uangamizwe, je umetuitia maneno haya!" (Bukhari). Na ilikuwa desturi yake kila mara kumfuata Mtume aendako na kuwaambia watu wasimsikilize, akisema, Mtume ni jamaa yake na ni mwehu. Kadhalika mkewe Abu Lahab aliyeitwa Ummi Jamil bint Harb, dada wa Abu Sufiyan, alikuwa mwanamke mbaya sana aliyekuwa anamwudhi sana Mtume na kumsumbua na hata kumsingizia-singizia mambo ya upuuzi. Na kwa sababu ya masingizio yake ameitwa *mchukuzi wa kuni* (Bukhari), ambazo kwazo amejikokea moto wa Jahanamu, (Razi).

سُوْرَةُ الْاِخْلَاصِ مَكِّيَّةٌ وَّ هِيَ مَعَ الْبَسْمَلَةِ خَمْسُ اٰيَاتٍ وَّ رُكُوْعٌ

112. SURA AL-IKHLAAS

Imeteremshwa Makka

Ina Aya 5 pamoja na Bismillahi

بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ ①

1. Kwa jina la Allah, Mwingi wa rehema, Mwingi wa ukarimu.

قُلْ هُوَ اللّٰهُ اَحَدٌ ②

2. Sema: Yeye Allah ni Mmoja.

اَللّٰهُ الصَّمَدُ ③

3. Allah Asiyehitaji, Ambaye wote wanahitaji Kwake.

لَمْ يَلِدْ ۙ وَلَمْ يُوْلَدْ ④

4. Hakuzaa wala Hakuzaliwa.

وَلَمْ يَكُنْ لَّهٗ كُفُوًا اَحَدٌ ⑤

5. Wala Hana anayefanana naye hata mmoja.

Sura hii ni katika sura za mwanzo kabisa kushuka Makka na mafundisho yake yanavunja kabisa ibada ya masanamu na Ukristo na kila mafundisho ya miungu wengi.

Aya 2. *Ahad* "Mmoja." Katika kiarabu neno *Ahad* ni tofauti na *Waahid* (mmoja). *Ahad* maana yake: Mmoja, Yeye tu, Peke Yake; na hakuna ye yote ajaye nyuma Yake wala aliyetangulia mbele Yake. Neno *waahid* hufuatwa na *mbili*, *tatu* n.k.w.; lakini *Ahad* halifuatwi na neno lo lote na ni sifa ya Allah tu. Hivi ndivyo ulivyo uzuri wa maneno ya Kiarabu na ukamilifu wa lugha hii. Neno *Ahad* linakataa kabisa fikira ya kusema kuna nafsi ya pili au ya tatu katika Uungu kama wasemavyo Wakristo.

Aya 3. *Samad*, "asiyehitaji ambaye wote wanahitaji Kwake," ni neno lenye maana hizi: (1) mkuu anayeendewa na watu kwa haja ya mambo yaliyo muhimu; (2) akaaye daima; (3) mwenye shani kubwa; (4) asiye na haja (Munjid); (5) mkuu mkubwa asiye na mipaka kwa ukubwa wake (Bukhari).

Bibi Aisha anasimulia ya kwamba Mtume *s.a.w.* alipokuwa akienda kitandani kwake kila usiku, aliunganisha vitanga vya mikono yake, kisha akavisomea *Qul huwallaahu* na *Qul a'uudhu birabbil falaq* na *Qul a'uudhu birabbinnaas*, na akavipulizia, kisha akavipaka mwili wake wote kila alipoweza kupagusa toka kichwani; na akifanya hivyo mara tatu (Bukhari jalada la 3).

سُوْرَةُ الْفَلَقِ مَدَنِيَّةٌ وَّ هِيَ مَعَ الْبَسْمَلَةِ سِتُّ اٰيَاتٍ وَّ رُكُوْعٌ

113. SURA AL-FALAQ

Imeteremshwa Madina

Ina Aya 6 pamoja na Bismillahi

بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ ①

1. Kwa jina la Allah, Mwingi wa rehema, Mwingi wa ukarimu.

قُلْ اَعُوْذُ بِرَبِّ الْفَلَقِ ۙ ②

2. Sema: Najikinga kwa Mola wa mapambazuko,

مِنْ شَرِّ مَا خَلَقَ ۙ ③

3. (Anilinde) katika shari ya Alivyoviumba,

وَ مِنْ شَرِّ غَاسِقٍ اِذَا وَقَبَ ۙ ④

4. Na katika shari ya giza la usiku liingiapo,

وَ مِنْ شَرِّ النَّفّٰثٰتِ فِي الْعُقَدِ ۙ ⑤

5. Na katika shari ya wale wanaopulizia mafundoni,

وَ مِنْ شَرِّ حَاسِدٍ اِذَا حَسَدَ ع ⑥

6. Na katika shari ya hasidi anapohusudu.

Sura hii ilishuka Madina. Masimulizi yanayoelezwa na baadhi ya wafasiri juu ya sababu za kushuka kwa sura hii, hayapatikani katika hadithi zilizo sahihi, hivyo hayakubaliwi.

Aya 3. *Shari ya Alivyoviumba.* Vitu vyote vilivyoumbwa vimeumbwa kwa ajili ya heri. Lakini pengine vinakuwa shari kama vitumiwe vibaya. Hivyo tumefundishwa tuombe tuepushwe na ubaya huu. Pengine inasemwa shari hiyo ni Shetani ambaye anaweza kuleta madhara makubwa, basi tunaomba ili tulindwe na shari yake. Pengine shari hii ni Jahanamu.

Aya 4. *Ghaasiq*, "Giza la usiku," ni kila kitu kinachotia giza katika moyo wa mtu na kinachomzuia kufuata mwongozo au kupata njia ya raha na neema.

Aya 5. *Wanaopulizia mafundoni,* maneno haya yametumiwa kwa *lugha ya fumbo* kuonyesha watu wanaotia vizuizi katika shauri au kazi ya mtu isimalizike, na wanaopulizia wasiwasi na maoni mabaya, au uadui katika *mafundo* yaani mafundo ya urafiki, udugu, mapatano ya kazi au ujamaa, ili kutokee kutosikilizana na machafuko.

Aya 6. *Hasidi* ni mtu mwenye husuda ambaye hutaka kupata kitu kile kile kilichoko kwa mtu mwingine kiwe kwake yeye na yule mwenye nacho akikose. Tunafundishwa hapa tulindwe na tabia hii mbaya inayomchukiza sana Allah. Mtume *s.a.w.* alisema: "Jiepusheni na husuda, maana husuda inakula wema kama moto unavyokula kuni" (Abu Dawud). Pia Mtume *s.a.w.* akasema, "Husuda ndio ugonjwa unaohilikisha mataifa" (Tirmidhi).

سُوْرَةُ النَّاسِ مَدَنِيَّةٌ وَّ هِىَ مَعَ الْبَسْمَلَةِ سَبْعُ اٰيَاتٍ وَّ رُكُوْعٌ

114. SURA AN-NAAS

Imeteremshwa Madina

Ina Aya 7 pamoja na Bismillahi

بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ ۝١

1. Kwa jina la Allah, Mwingi wa rehema, Mwingi wa ukarimu.

قُلْ اَعُوْذُ بِرَبِّ النَّاسِ ۝٢ۙ

2. Sema: Ninajikinga kwa Mola wa watu,

مَلِكِ النَّاسِ ۝٣ۙ

3. Mfalme wa watu,

اِلٰهِ النَّاسِ ۝٤ۙ

4. Mwabudiwa wa watu,

مِنْ شَرِّ الْوَسْوَاسِ ۙ الْخَنَّاسِ ۝٥ۙ

5. Katika shari ya wasiwasi wa (Shetani) aendaye kisirisiri kwa hila,

الَّذِىْ يُوَسْوِسُ فِىْ صُدُوْرِ النَّاسِ ۝٦ۙ

6. Atiaye wasiwasi mioyoni mwa watu,

مِنَ الْجِنَّةِ وَالنَّاسِ ۝٧ع

7. Miongoni mwa majini na watu. ع ١ ٧ ٣٩

Sura hii ilishuka Madina, ingawa baadhi ya wanazuoni wanasema ilishuka Makka.

Aya 2. *Rabb,* "Mola." Maana ya neno hili ni Mwumba, Mola, Bwana, na anayelea kwa taratibu na kufikisha kitu katika ukamilifu wake. Pia maana yake ni akusanyaye, anayehukumu, anayekamata na anayestahili kutiiwa (Akrab, Lisan na Mufradat).

Aya 5. *Khannaas,* "aendaye kisirisiri kwa hila," yaani Shetani. Pia asemaye maneno maovu anaitwa *khannaas*. Kadhalika *khannaas* ni mtu atiaye wasiwasi katika nyoyo za watu na anawazuia wawe nyuma.

Sura hii ni sura ya mwisho ya Qur'an, inayotufundisha ya kuwa kila mara tumuombe Allah tuzingatie heri nyingi iliyoshuka katika Qur'an kwa namna ya mafundisho na hekima na methali ya watu wema ili tuongoke, na tupate radhi ya Allah na heri hizo zisitutoke mikononi mwetu.

Pia tumefundishwa ya kuwa katika siku za mwisho, kama vile sura hizi zinavyotabiri habari za siku za mwisho, fitina za namna mbalimbali zitatokea, na hatuwezi kusalimika pasipo msaada wa Allah. Watu wasijitegemee kwa uwezo wao tu bali wamtegemee Allah kwa kumwomba msaada.

Tumeagizwa tutakapoanza kusoma Qur'an tusome *A'uudhu billaahi minashshaitaanir-rajiim* ili tusizuiliwe kupata heri zilizomo ndani ya Qur'an. Na mwisho zimewekwa sura mbili za *a'uudhu* ili heri tulizokwisha pata zisitutoke.

DUA BAADA YA KUMALIZA QUR'AN

اَللّٰهُمَّ ارْحَمْنِیْ بِالْقُرْاٰنِ الْعَظِیْمِ وَاجْعَلْهُ لِیْٓ اِمَامًا وَّ نُوْرًا وَّ هُدًی وَّرَحْمَةً.
اَللّٰهُمَّ ذَكِّرْنِیْ مِنْهُ مَانَسِیْتُ وَعَلِّمْنِیْ مِنْهُ مَاجَهِلْتُ وَارْزُقْنِیْ تِلَاوَتَهٗٓ
اٰنَآءَ الَّیْلِ وَالنَّهَارِ وَاجْعَلْهُ لِیْ حُجَّةً یَّارَبَّ الْعَالَمِیْنَ.

Ee Allah, niondolee hofu yangu katika kaburi langu. Ee Allah, nirehemu kwa Qur'an hii iliyo tukufu na Uifanye iwe kwangu kiongozi na nuru, na mwongozo na rehema. Ee Allah, Unikumbushe ya humo niliyoyasahu, na Unifundishe ya humo nisiyoyajua, na Uniruzuku (uwezo wa) kuisoma nyakati za usiku na mchana, na Uifanye iwe kwangu hoja, Ewe Mola wa walimwengu. Amin.